


Tarjuma ya
Qur'ani Tukufu



Islamic Information Center
Msikiti Mkuu wa Sultan Qaboos
Sultanate of Oman

Tarjuma ya
Qur'ani Tukufu

**Tarjuma hii inatokana kwa ukamilifu
na tarjuma ya Al Muntakhab iliyo
tarjimiwa na -**

Sheikh Ali Muhsin Al Barwani

**Islamic Information Center
Msikiti Mkuu wa Sultan Qaboos
Sultanate of Oman**

Imetayarishwa na kuchapishwa na

**Islamic Information Center
Msikiti Mkuu wa Sultan Qaabus, Muscat
Sultanate of Oman
www.iicomman.com
info@iicomman.com**

Chapa ya kwanza: September 2023



Kitabu hichi hakiuzwi

Yaliyomo

| Sura | | Ukurasa |
|------|------------------------|---------|
| | Dibaji ya Mchapishaji | i |
| | Utangulizi | ii |
| | Uhalisi wa Qur'ani | iv |
| 1 | Al-Faatih'a | 1 |
| 2 | Al-Baqara | 3 |
| 3 | Al I'mran | 55 |
| 4 | An-Nisaa | 84 |
| 5 | Al-Maida | 114 |
| 6 | Al-An'am | 137 |
| 7 | Al-A'raaf | 164 |
| 8 | Al-Anfaal | 194 |
| 9 | At-Tawba | 206 |
| 10 | Yunus | 227 |
| 11 | Hud | 243 |
| 12 | Yusuf | 261 |
| 13 | Ar-Ra'ad | 278 |
| 14 | Ibrahim | 286 |
| 15 | Al-Hijr | 293 |
| 16 | An-Nah'l | 301 |
| 17 | Al-Israa (Bani Israil) | 320 |
| 18 | Al-Kahf | 334 |
| 19 | Maryam | 348 |
| 20 | T'aha | 358 |
| 21 | Al-Anbiyaa | 371 |
| 22 | Al-Hajj | 383 |
| 23 | Al-Muuminun | 395 |
| 24 | An-Nur | 406 |
| 25 | Al-Furqan | 417 |
| 26 | Ash-Shu'araa | 427 |
| 27 | An-Naml | 442 |
| 28 | Al-Qasas | 453 |
| 29 | Al-'Ankabut | 465 |
| 30 | Ar-Rum | 475 |
| 31 | Luqman | 483 |
| 32 | Assajdah | 488 |
| 33 | Al-Ah'zab | 492 |
| 34 | Saba' | 503 |
| 35 | Faat'ir | 511 |
| 36 | Ya-Sin | 519 |

| Sura | | Ukurasa |
|-------------|---------------------------|----------------|
| 37 | Ass'affat | 527 |
| 38 | S'aad | 539 |
| 39 | Azzumar | 547 |
| 40 | Ghaafir (Al-Muumin) | 558 |
| 41 | Fuss'ilat (Ha Mim Sajdah) | 569 |
| 42 | Ash-Shuura | 577 |
| 43 | Azzukhruf | 585 |
| 44 | Addukhan | 594 |
| 45 | Al-Jaathiya | 599 |
| 46 | Al-Ah'qaaf | 604 |
| 47 | Muh'ammad | 610 |
| 48 | Al-Fat'h | 615 |
| 49 | Al-H'ujuraat | 620 |
| 50 | Qaaf | 623 |
| 51 | Adh-Dhaariyaat | 627 |
| 52 | Att'ur | 632 |
| 53 | Annajm | 636 |
| 54 | Al-Qamar | 641 |
| 55 | Arrah'man | 645 |
| 56 | Al-Waaqia'h | 650 |
| 57 | Al-H'adiid | 656 |
| 58 | Al-Mujaadalah | 662 |
| 59 | Al-H'ashri | 666 |
| 60 | Al-mumtah'inah | 670 |
| 61 | Ass'af | 674 |
| 62 | Al-Jumua' | 677 |
| 63 | Al-Munaafiqun | 679 |
| 64 | Attaghaabun | 681 |
| 65 | Att'alaq | 684 |
| 66 | Attah'riim | 687 |
| 67 | Al-Mulk | 690 |
| 68 | Al-Qalam | 694 |
| 69 | Al-H'aaqqah | 698 |
| 70 | Al-Maa'rij | 702 |
| 71 | Nuh' | 706 |
| 72 | Al-Jinn | 709 |
| 73 | Al-Muzzammil | 712 |
| 74 | Al-Muddaththir | 715 |
| 75 | Al-Qiyamah | 719 |
| 76 | Al-Insan | 722 |
| 77 | Al-Mursalaat | 725 |

| Sura | | Ukurasa |
|-------------|----------------------|----------------|
| 78 | An-Naba' | 729 |
| 79 | An-Nazi'at | 732 |
| 80 | 'Abasa | 735 |
| 81 | Attakwir | 738 |
| 82 | Al-Infit'aar | 740 |
| 83 | Al-Mut'affifin | 742 |
| 84 | Al-Inshiqaaq | 745 |
| 85 | Al-Buruuj | 747 |
| 86 | Att'aariq | 749 |
| 87 | Al-A'ala | 751 |
| 88 | Al-Ghaashiyah | 753 |
| 89 | Al-Fajr | 755 |
| 90 | Al-Balad | 757 |
| 91 | Ash-Shams | 759 |
| 92 | Al-Layl | 761 |
| 93 | Adh-Dhuh'aa | 763 |
| 94 | Ash-Sharh' | 764 |
| 95 | At-Tin | 765 |
| 96 | Al-'Alaq | 766 |
| 97 | Al-Qadr | 768 |
| 98 | Al-Bayyinah | 769 |
| 99 | Az-Zilzalah | 771 |
| 100 | Al-'Aadiyaat | 772 |
| 101 | Al-Qaari'ah | 773 |
| 102 | At-Takaathur | 774 |
| 103 | Al-'As'r | 775 |
| 104 | Al-Humazah | 776 |
| 105 | Al-Fiil | 777 |
| 106 | Quraish | 778 |
| 107 | Al-Maa'u'n | 779 |
| 108 | Al-Kawthar | 780 |
| 109 | Al-Kaafirun | 781 |
| 110 | An-Nas'r | 782 |
| 111 | Al-Masad | 783 |
| 112 | Al-Ikhlash' | 784 |
| 113 | Al-Falaq | 785 |
| 114 | An-Naas | 786 |
| | Maelezo Zaidi ya Aya | 788 |
| | Orodha ya Maneno | 855 |

Dibaji ya Mchapishaji

Qur’ani imeteremshwa kwa lugha ya Kiarabu, na Waislamu wote duniani wanaisoma kwa lugha hiyohiyo kwa sababu neno na maana ya aya za Qur’ani zinatoka kwa Mwenyzi Mungu. Lengo la tarjuma na tafsiri ya Qur’ani kwa lugha nyengine ni kusaidia watu wasiojuwa Kiarabu kuufahamu ujumbe wa Mwenyzi Mungu.

Qur’ani ya Kiarabu ni moja tu, hakuna ya pili, lakini tarjuma na tafsiri za Qur’ani hata katika lugha moja zinaweza kutafautiyana. Na hii ni kwa sababu mbili:

Kwanza, maneno ya Kiarabu ni mapana katika maana zake na maranyigine hutumika kama ni mithali (*figuratively*). Kwahivyo tarjuma inategemeya ufahamu na maoni ya mutarjim na uamuzi wake wa kuchagua maneno katika lugha.

Pili, katika baadhi ya aya za Qur’ani, tarjuma na tafsiri za Qur’ani mbali mbali hutafautiana kwa mujibu wa msimamo wa wafasiri katika kanuni za imani. Kwa mfano, wafasiri wanatafautiana katika aya zinazohusu Kuonekana kwa Mwenyzi Mungu akhera, au kuwekwa Motoni waumini walio fanya dhambi kwa muda maalumu tu, au kuwa Mwenyzi Mungu ana mwili na viungo. Tafauti hizi ni chache na ziko katika eneo la wataalamu wa kanuni za imani.

Katika tarjuma hii, kila aya ina tanbihi (*footnote*) ambayo ni tafsiri ya hiyo aya, na baadhi ya aya pia zina maelezo zaidi ambayo yamewekwa mwisho wa kitabu.

Mutarjim wa Qur’ani hii ametumiya lugha ya Kiswahili ya asili na kwa hivyo utakutana na maneno ambayo asili yake ni ya Kiarabu lakini pia ni maneno ya Kiswahili asili; Kwa mfano, dabiri (*organize*), ghurika (*deceive*), zahama (*chaos*), na mengineo.¹ Baadhi ya maneno ambayo sio ya kawaida katika lugha ya Kiswahili yamefafanuliwa katika ‘Orodha ya Maneno’ mwisho wa kitabu.

¹ Tazama “Comprehensive Swahili-English Dictionary” by Mohamed A Mohamed, EAEP.

Utangulizi

Qur'ani ni maandiko yaliotoka kwa Allah alioteremshiwa Mtume Muhammad (*Salaa na amani za Allah zimfikiye*) kupitia kwa Malaika Jibril. Qur'ani ni ufunuo wa mwisho kutoka kwa Allah kwa wanadamu wote mpaka mwisho wa dunia. Qur'ani imeteremshwa kuukamilisha ujumbe wa Allah kwa wanadamu, kuthibitisha yaliyoteremshwa kabla yake na kusahihisha mabadiliko yaliyo ingizwa ndani ya mabaki ya vitabu vilivyopita.

Kuteremshwa kwake

Qur'ani iliteremshwa kidogo kidogo kwa hatua, katika lugha ya Kiarabu, kwa muda wa miaka 23, kuanzia mwaka 610 mpaka 632 CE. Huku kuteremshiwa Qur'ani kidogo kidogo kuliwaletea waumini muongozo wa kupangilia kwa mujibu wa hali maalumu zinazotokezeya. Pia ilihakikisha kuwaingia watu sheria za Allah vizuri na kutekelezwa vizuri katika maisha ya waumini.

Kusajiliwa na kuhifadhiwa kwake

Kila anapo pokea ufunuo, Mtume (*Salaa na amani za Allah zimfikiye*) alikuwa akiwaamuru waandishi wake waandike yaliyoteremshwa, huku na yeye akishuhudia na kusimamia. Wakati huo huo, Mtume na wengi katika masahaba zake, wa kiume na wa kike, walidhihifadhi kwa moyo aya hizo kama zilivyoteremshwa. Kwa njia hii Qur'ani iliandikwa na kuhifadhiwa moyoni na waumini wa kiume na kike katika wakati wa uhai wa Mtume. Mazoezi ya kuhifadhi moyoni Qur'ani yanaendelea mpaka hivi leo. Wakati wowote ule katika historia ya Uislamu wapo mamilioni ya Waislamu ambao wamehifadhi Qur'ani nzima katika maandishi yake asili na halisi. Leo inakisiwa kuwepo zaidi ya Waislamu milioni ishirini ambao wamehifadhi Qur'ani kamili, na mamilioni wengine wamehifadhi sehemu kadha ya Qur'ani.

Yaliyomo na dhamira yake

Qur'ani ina sura 114. Idadi ya aya zilizomo ndani ya sura inatafautiana, kuanzia aya 3 (Sura ya 103 na 108) mpaka aya 286 (Sura ya 2). Qur'ani ni kitabu cha muongozo, onyo na mabashirio mema, na pia chenye maelezo ya umma zilizopita na watume wake. Kwa ujumla inagusia dhamiri nne:

Kwanza: Inatueleza kuhusu Allah; Jinsi yake na Sifa zake. Kwa mfano, Sura ya 112 inaeleza Upekee wa Mungu (*Tawheed*) na sifa Zake za pekee ambazo hazina ushirika na mwengine yoyote.

Pili: Inaelezea juu ya uhusiano baina yetu na Allah; kwa nini alituumba na nini wajibu wetu Kwake. Kwa mfano, Allah anasema katika Qur’ani, sura ya 51, aya ya 56:

Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.

Katika aya hii, neno ‘*ibada*’ linamaanisha kumtumikia Mwenyezi Mungu Muumba na kuishi kwa kufuata maamrishi Yake. Tena Qur’ani inaelezea juu ya uhusiano baina yetu na viumbe vyengine vilivyobakia; Malaika, Majini, ulimwengu wa wanyama na dunia yote; nini umuhimu na maingiliano yao kwenye uhai wetu.

Tatu: Inatoa muongozo kwa kuweka sheria na kuonesha njia iliyosawa, na inaweka nguzo na kipimo cha tabia njema za maisha. Inaahidi pepo ya milele kwa wale wanaofuata muongozo huu na inaahidi mateso ya milele kwa wale wenye kwenda kinyume na muongozo huu.

Mwishowe, Qur’ani inatuambia kuwa umma zote zilizopita zilipewa muongozo kupitia kwa mitume. Kwa mfano, katika sura ya 10, aya ya 47 Allah anasema:

Na kila umma una Mtume. Alipo wajia Mtume wao walihukumiwa baina yao kwa uadilifu, wala hawakudhulumiwa.

Maalezo ya umma zilizopita ni kisomo kwa wanadamu juu ya matokeo ya vitendo vya umma hizo. Kwa mfano, Qur’ani inatuhadithia juu ya shida aliyopata Mtume Nuh kwa watu wake na mafuriko yaliyofuatia. Inatuhadithia juu ya shida aliyopata Mtume Musa kwa watu wake na kwa Firauni. Na tena kuna “bora ya hadithi zote”, hadithi ya maisha ya Mtume Yusuf. Kwa ujumla, Qur’ani inaelezea hadithi za watume 25 kati ya maelfu ambao Allah aliwatuma kwa wanadamu katika zama zote.

Islamic Information Center
Msikiti Mkuu wa Sultan Qaboos
Sultanate of Oman

Uhalisi wa Qur’ani

Jee, hali Qur’ani ni kweli ufunuo unaotoka kwa Mwenyezi Mungu? Hili ni suala la halali, kwa sababu leo duniani kuna maandiko mengi, ambayo yanapingana katika yaliyomo, na bado kila moja inadai kuwa imetoka kwa Mungu. Kuongezea katika suala hili, baadhi ya watu wanaweza kuuliza: Tuna uhakika gani kuwa Qur’ani haikubadilishwa kupitia miaka yote hiyo iliyopita? Majibu ya masuala haya yanapatikana katika Qur’ani yenyewe, ambayo imetoa vigezo vitatu (au hoja tatu) za kuufafanua ukweli.

Kigezo cha kwanza

Ufunuo wa kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu umefungamana kwa ukamilifu, na hauna hitilafu yoyote ndani yake, (Tazama Sura ya 4, Aya ya 82). Maandiko yoyote yenye hitilafu au kuwa na makosa ndani yake hayawezi kutokana na Mwenyezi Mungu. Qur’ani kamwe haina hitilafu wala utata. Hii pia inathibitisha kuwa haikubadilishwa na mikono ya mtu kupitia miaka yote.

Kigezo cha pili

Ufunuo wa kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu unapindukia uwezo wa mwanadamu katika kutimiza mahitajio ya mwanadamu kwa marefu na mapana; katika sheria, uadilifu, murua na muongozo wa kiroho, na pia una nguvu za mijadala, hoja, ufasihi wa maneno na mtindo. Kwa hivi, Allah amempa mwanadamu changamoto ya kuleta kitabu japo cha kufanana na Qur’ani. (Tazama Sura ya 2, Ayay ya 23 – 24, na Sura ya 17, Aya ya 88). Ni pekee Muumba Mwenye Ujuzi wa Yote anayeweza kutoa changamoto hii. Ingelikuwa Qur’ani imepata kubadilishwa na mtu, wangaliweza watu wengine kutoa kitabu chenye kufanana nacho. Changamoto hii imesimama mpaka leo kama ilivyo simama miaka 1400 iliyopita.

Kigezo cha tatu

Ufunuo unaotoka kwa Mwenyezi Mungu ni lazima uwe unafaa na kutumika wakati wote na ubakie wenye kukubaliana na ilimu ya mwanadamu kila inapoendelea, na mahitajio ya mwanadamu yanavyobadilika na kukua. Kanuni za Qur’ani katika sheria, haki, biashara, nidhamu ya jamii na tabia njema zinafaa na kutumika leo kama zilivyokuwa zaidi ya miaka 1400 iliyopita wakati Qur’ani ilipoteremshwa. Na zaidi ya hayo, Qur’an inakubaliana kamili na kila pande za ilimu ya kisasa katika sayansi za maumbile.

Ingelikuwa Qur’ani imetokana na mtu, sio Mwenyezi Mungu, au ingelibadilishwa, basi kufaa na kutumika kwake leo kungelipotoka na kusingewezekana. Kwa milele Qur’ani itafaa na kutumika katika kila pande za ilimu ya mwanadamu na mahitajio yake.

Vigezo hivi, pamoja na mengine yaliyomo ndani ya Qur’ani, vyote vyenye athari nzito na nguvu za kutosheleza mahitajio ya mwanadamu na muongozo, vinadhahirisha na kuthibitisha muujiza wa Qur’ani. Kwa hakika Qur’ani ni muujiza pekee alioudai Mtume Muhammad (*Salaa na amani za Allah zimfikiye*).

Sura 1 - Al Faatih'a

Utangulizi

Sura hii iliteremka Makka kabla ya Hijra, kuhamia Mtume s.a.w. Madina. Imeitwa Al-Faatih'a, yaani Kifungulio kwa kuwa ndiyo sura ya mwanzo katika mpango wa Msahafu Mtukufu, nayo ni sura ya mwanzo iliyo teremka kwa utimilivu wake. Na sura hii inakusanya jumla ya yaliyomo katika Qur'ani na kama kwamba huu ni mukhtasari wake, na baadaye yatakuja mambo kwa tafsili, babu-babu.

Na makusudio ya Qur'ani ni: Kubainisha Tawhid, Upweke wa Mwenyezi Mungu; na kubainisha ahadi na bishara kwa Muumini mtenda mema; na kubainisha ahadi na onyo kwa kafiri na mtenda maovu; na kubainisha ibada; na kubainisha njia ya kufanikiwa duniani na Akhera; na hadithi za walio mt'ii Mwenyezi Mungu wakafuzu, na hadithi za walio muasi wakaangamia.

Sura Al-Faatih'a inakusanya kwa ufupi na kwa kuashiria makusudio haya, na kwa hivyo ndio ikaitwa pia "Ummul Kitaab" yaani "Msingi wa Kitabu".

*** **

1. KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.¹

2. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote;²

3. Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu;³

4. Mwenye Kumiliki Siku ya Malipo.⁴

5. Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada.⁵

6. Tuongoe njia iliyo nyooka,⁶

7. Njia ya ulio waneemesha, siyo ya walio kasirikiwa, wala walio potea.⁷

1 Sura inaanza kwa Jina la Mwenyezi Mungu ambaye hapana anayefaa kuabudiwa ila Yeye aliye sifika kwa kila sifa za ukamilifu, na ametakasika na kila la upungufu. Yeye ndiye Mwenye rehema ambaye ananeemesha kwa neema kubwa na ndogo, na za kuwapa wote, na za kuwapa walio khusika. Na Yeye ndiye mwenye kusifika kwa sifa ya Rehema yenye kudumu. (Kauli ya mwanzo aliyo semezwa Mtume s.a.w. na kuamrisha na Mwenyezi Mungu ni "*Iqra` bismi Rabbika*", yaani: "Soma kwa jina la Mola wako Mlezi!" Naye Mtume s.a.w. amesema: "Jambo lolote lisilo anziwa kwa *Bismillahi* ni pungufu." Kila Sura ya Qur'ani, isipo kuwa Sura Attawba, imeanziwa kwa *Bismillahi Rrahmani Rrahim*.)

2 Sifa njema za namna yote na katika kila hali ni za Mwenyezi Mungu pekee. Na tunamsifu Yeye kwa sifa zote kwa sababu Yeye ndiye mwenye kuvumba viumbe vyote na mwenye kuviangalia na kuvilea. (Neno Rabb, kwa Kiarabu, lina maana ya Ubwana na Ulezi na Utengenezaji. Ndiyo tukatumia Mola Mlezi. Neno Baba lina upungufu.)

3 Na Yeye ndiye Mwenye rehema ya kudumu, na rehema inatokana naye. Ananeemesha kwa neema zote ndogo na kubwa. (*Arrahman* ni jina lake Mwenyezi Mungu tu, na hafai mtu kuitwa hivyo.)

4 Na Yeye peke yake ndiye Mwenye kumiliki Siku ya Malipo na Hisabu, yaani Siku ya Kiyama, anafanya atakavyo wala hapana mwenye kushirikiana naye walau kwa kuonekana tu.

5 Hatumuabudu yeyote ila Wewe tu, wala hatutaki msaada kwa yeyote ila kwako tu.

6 Tunakuomba utuwafikishe kuendea Njia ya haki, na kheri na mafanikio.

7 Na njia hiyo ndiyo ya waja wako ulio wawezesha kukuamini Wewe, na ukawajaalia neema ya uwongofu na radhi, sio njia ya walio stahiki kupata ghadhabu zako na wakaiwacha njia ya haki na kheri, kwa sababu hao wameitupa imani kukuamini Wewe na kuelekea kwenye uwongofu wako. (*Tazama Maelezo 1:7*)

Sura 2 - Al-Baqara

Utangulizi

Sura hii imeteremka Madina baada ya Hijra. Nayo ndiyo sura ndefu kuliko zote katika Qur'ani Tukufu kwa mujibu wa mtungo wa Msahafu. Sura hii imeanzia kueleza kwa tafsili yale yaliyo malizikia Sura ya Al Faatiha. Imetaja kuwa Qur'ani ndiyo msingi wa uwongofu, na imewataja wale walio neemeshwa na Mwenyezi Mungu kwa kupata radhi zake, na wale walio kasirikiwa, nao ni makafiri na wanaafiki.

Sura imeeleza ukweli wa Qur'ani, na kwamba wito wake ni wa kweli usio na shaka. Kisha ikaingia kueleza namna tatu za watu: Waumini, Makafiri na Wanaafiki. Na ikataja Daa'wa, Mlingano, au Wito, kuwaita watu wamuabudu Mwenyezi Mungu pekee, na ikawaonya makafiri, na ikawapa bishara njema Waumini. Baadaye ikawaelekea Wana wa Israili khasa kwa kuwaita na kuwakumbusha siku za Mwenyezi Mungu, na kwa vituko vyao na Musa a.s. na kuwakumbusha khabari za Ibrahim na Ismail na walivyo ijenga *Al Kaaba*. Hayo yamechukua karibu nusu ya Sura. Mazungumzo yakawageukia Waumini wazingatie yaliyo wapata Mayahudi na Wakristo.

Mazungumzo yakaingia kuwasemeza watu wa Qur'ani kwa kuwakumbusha mambo ambayo umma wa Musa na umma wa Muhammad walivyo shirikiana katika kutukuzwa Ibrahim na kuongoka kwake na nasaba yake, na kwa kutaja *kibla* na mfano wa hayo.

Kisha yakaja mazungumzo juu ya Tawhid (Upweke wa Mwenyezi Mungu) na kukumbusha Ishara za Mwenyezi Mungu zenye kumuashiria Yeye. Na yakaja masimulizi juu ya ushirikina, na juu ya vyakula vilivyo harimishwa, na kwamba kuharimisha na kuhalalisha ni haki ya Mwenyezi Mungu peke yake.

Sura ikaingia kubainisha misingi ya wema, na kutaja baadhi ya hukumu za Saumu, na wasia, na kula mali ya watu kwa dhulma, na kisasi, na vita, na Hija, na ulevi, na kamari, na ndoa na talaka, na kunyonyesha, na eda na mengineyo. Hali kadhaalika yamezungumzwa mambo ya itikadi kwa jumla kama Utume, Tawhidi, kufufuliwa. Yametajwa mas-ala ya kutoa sadaka na Zaka, riba, biashara, kuandikiana madeni. Mwishoe Sura yakhitimisha kwa dua ya Waumini kumwomba Mola wao Mlezi awanusuru na awasaidie.

Sura hii imekusanya misingi kadhaa wa kadhaa. Miongoni mwayo ni:

Kwamba Njia ya Mwenyezi Mungu na kuishika Dini yake ni dharura kwa ajili ya kupata mafanakio duniani na Akhera, na kwamba haielekei kwa mwenye akili kuwaita watu watende mema naye akajisahau mwenyewe; na ya kwamba yapasa kuchagua kheri kuliko shari, na kukhiari lilio bora kuliko lilio duni.

Na kwamba misingi ya Dini ni mitatu, nayo ni: Kumuamini Mwenyezi Mungu, Kuamini kufufuliwa, na Kutenda mema.

Na kwamba malipo ni kwa Imani na vitendo pamoja. Shuruti ya Imani ni kukiri kwa nafsi na kukubali kwa moyo kila alilo kuja nalo Mtume s.a.w., na kwamba wasio kuwa Waislamu hawatokuwa radhi na Waislamu mpaka Waislamu wafuate dini yao hao walio potea.

Na kwamba kwa jumla urafiki katika sharia yapasa uwe kwa wenye kushika Imani na uadilifu, sio kwa watu wa kufuru na dhulma, na kwamba Imani ya Dini ya Mwenyezi Mungu inalazimisha uwepo umoja na kuwafikiana, na kutofuata hayo huleta khitilafu

na kutengana. Kwa ajili ya kupata mambo makuu inalazimu kutafuta msaada kwa Subira na Sala. Kufuata kipofu-pofu ni upotovu, na hupelekea ujinga na chuki za kitaifa.

Na kwamba Mwenyezi Mungu amewahalalishia waja wake vyakula vizuri na amewaharimishia vichache vilivyo viovu; wala haijuzu kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu kuhlalisha au kuharimisha kitu. Na vilivyo harimishwa huhalalishiwa mwenye dharura, kwa sababu dharura huruhusu vilivyo katazwa, na dharura hupimwa kwa kadiri yake. Dini imejengwa juu ya wepesi na kuondoa mikazo. Kwani Mwenyezi Mungu hailazimishi nafsi ila kwa kiasi ya uwezo wake, wala hawaamrishi waja wake ila kwa wanalo liweza. Ni haramu, haijuzu mtu kujipelekea nafsi yake kwenye maangamizo. Kila jambo hutafutwa kwa sababu zake na njia zake zitakao fikilia. Kulazimisha katika dini kunakatazwa. Kupigana vita ni kwa ajili ya kujilinda, na kwa ajili ya kuhifadhi uhuru wa dini, na kuulinda utukufu wa Uislamu katika miji yake.

Na kwamba Muislamu anayo haki ya kutaka sehemu yake katika dunia, kama anavyo tekeleza wajibu wake kwa ajili ya Akhera, na kwamba kutimiza haja na kuleta maslahi ni miongoni mwa makusudio ya Sharia.

Na kwamba Imani na Subira ni sababu mbili zinazo wapelekea wachache walio waadilifu kuwashinda wengi wenye kudhulumu, na kula mali ya watu kwa upotovu ni haramu, na mwanaadamu analipwa kwa vitendo vyake mwenyewe si kwa vitendo vya mwengine, na hikima ya utungaji sharia inafahamiwa na akili iliyo kaa sawa kwa kuwa ndani yake mna haki na uadilifu na maslahi ya waja.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Mim.¹

2. Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uwongofu kwa wachamungu,²

3. Ambao huyaamini ya ghaibu na hushika Sala, na hutoa katika tuliyo wapa.³

4. Na ambao wanayaamini yaliyo teremshwa kwako, na yaliyo teremshwa kabla yako; na Akhera wana yakini nayo.⁴

1 Alif Lam Mim: Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taala* ameanzia kwa harufi hizi kuashiria moja katika miujiza ya Qur'ani Tukufu iliyo tungwa kwa harufi zile zile ambazo Waarabu wakitungia maneno yao, na juu ya hivyo wao wameemewa hawakuweza kuleta kitu mfano wa Qur'ani hii. Pia juu ya hivyo hizi harufi zinazindua ili upate kuzingatia yasemwayo.

2 Hichi ndicho Kitabu kilicho kamilika, kisicho kuwa na towa, nacho ni Qur'ani tunayo iteremsha isiyo tiliwa shaka yoyote na kila mwenye akili na mwenye insafu akajua kuwa inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Wala haitilii shaka kuwa yasemwayo juu ya mambo na hukumu ni ya kweli tupu. Ndani ya Kitabu hichi upo uwongofu ulio kamilika kwa walio kuwa tayari kuitafuta Kweli, na wanajikinga na madhara na mambo ya kuwaletea adhabu.

3 Na hawa ndio ambao, kwa kuazimia na kunyenyekea, wanayasadiki yale ya ghaibu wasio yaona kwa macho, wala kuyahisi kwa viungo, ambayo ni ya kuitakidiwa na kuaminiwa, kama mambo ya Malaika, Siku ya Akhera. Kwani msingi wa kushika Dini ni kuamini yaliyo ya ghaibu. Pia wakashika Sala vilivyo, kwa kumwelekea Mwenyezi Mungu na kumnyenyekea kikweli, na wale ambao wanatoa katika yale alio waruzuku Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mambo ya kheri na mema.

4 Na wale wanao isadiki Qur'ani ulio teremshiwa wewe (Muhammad) kutoka kwa Mwenyezi Mungu,

5. Hao wapo juu ya uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi, na hao ndio walio fanikiwa.⁵
6. Hakika wale walio kufuru ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawaamini.⁶
7. Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao, na juu ya macho yao pana kifuniko. Basi watapata adhabu kubwa.⁷
8. Na katika watu, wako wasemao: Tumemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, wala wao si wenye kuamini.⁸
9. Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walio amini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao; nao hawatambui.⁹
10. Nyoyoni mwao mna maradhi, na Mwenyezi Mungu amewazidishia maradhi. Basi watakuwa na adhabu chungu kwa sababu ya kusema kwao uwongo.¹⁰
11. Na wanapo ambiwa: Msifanye uharibifu ulimwenguni. Husema: Bali sisi ni watengenezaji.¹¹
12. Hakika wao ndio waharibifu, lakini hawatambui.¹²
13. Na wanapo ambiwa: Aminini kama walivyo amini watu. Husema: Tuamini kama

na yote yaliomo ndani yake katika mambo ya hukumu na khabari, na wakatenda yatakikanayo, na wakavisadiki Vitabu vya Mwenyezi Mungu walivyo teremshiwa Manabii na Mitume wa kabla yako, kama Taurati na Injili na vyenginevyo. Kwani risala za Mwenyezi Mungu zote zina asli moja, na hao wanatambulikana kuwa wanaamini Imani moja isiyo legalega ya Siku ya Kiyama na yatayo tokea ya Hisabu na Thawabu na Adhabu.

5 Hawa walio sifiwa kwa sifa zilizo tangulia, wametua kwa kupata sababu za uwongofu wa Mwenyezi Mungu, na wamekaa imara juu ya hayo. Wao peke yao ndio walio fuzu watakapata wayatakayo, na wayatamaniayo, nayo ni malipwa kwa kazi yao na juhudi yao, na kutimiza amri na kuepuka waliyo katazwa.

6 Hii ndiyo hali ya waongofu. Ama wajinga, majaahili, walio acha kujitayarisha kwa Imani kwa mapuuzi na kufanya inda, wasimwitikie Mwenyezi Mungu, basi ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye. 7 Ukafiri umesaki kwa watu hao, hata imekuwa kama nyoyo zao zimetwa muhuri, zimezibwa kwa vizibo, haziingii kitu chochote zaidi ya kiliomo ndani yake. Na kama kwamba masikio yao pia yamezibwa, hayasikii onyo lake la kweli, na kama kadhaalika wamefunikwa kwa vitanga vya macho. Hawazioni ishara za Mwenyezi Mungu zenye kuonyesha Imani. Kwa hivyo basi imekuwa wanastahiki kuwafikilia adhabu iliyo kali.

8 Na miongoni mwa makafiri wapo watu ambao husema kwa ndimi zao yasiyo kuwamo nyoyoni mwao. Hudhihirisha imani na kusema: “Sisi tunamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Kiyama,” na wala hawasemi kweli. Basi hao hawaingii katika kundi la Waumini.

9 Hao makafiri wadanganyifu huwakhadaa Waumini kwa wanayo yafanya, na wao hudhania kuwa wanamdanganya Mwenyezi Mungu. Wanafikiri kuwa Yeye hayajui wanayo yaficha, na kumbe Yeye anayajua ya siri na yanayo non’gonwa. Basi wao kwa hakika wanajikhadaa wenyewe, kwa sababu madhara ya vitendo vyao yatawapata wao, sasa au baadae. Mwenye kumkhadaa mtu, na akadhani kuwa huyo mtu hajui naye kumbe anajua, basi inakuwa anajikhadaa mwenyewe nafsi yake.

10 Katika nyoyo za watu hawa mna maradhi ya uhasidi na chuki kwa watu wa Imani, na itikadi zao zimefidsidika. Mwenyezi Mungu basi anawazidishia hayo maradhi yao, kwa ajili ya kuinusuru Haki, kwani hayo yanawaudhi wao kwa sababu ya uhasidi wao, na chuki yao, na inadi yao. Watu hao watapata adhabu iliyo chungu duniani na Akhera kwa sababu ya uwongo wao na upinzani wao.

11 Na pindi mmojawapo wa walio ongoka akiwaambia hawa wanaafiki: “Msifanye uharibifu katika nchi kwa kuinginga Njia ya Mwenyezi Mungu, na kuwasha fitna, na kuwasha moto wa vita,” wao hujitoa makosani mwa uharibifu, na husema: “Kee sisi ndio tunao tengeneza.” Na hayo ni kwa kuwa ghururi yao imepita mpaka. Huu ndio mwendo wa kila mharibifu, khabithi mwenye ghururi. Yeye hudai kuwa ule uharibifu wake ndio matengenezo na maendeleo.

12 Enyi Waumini! Amkeni, mtanabahi, muwatambue kuwa hao ndio mafisadi wa kweli, lakini wenyewe hawautambui ufasidi wao kwa ajili ya ghururi walio nayo, wala hawaitambui adhabu kali watakayo ipata kwa unaafiki wao huu.

walivyo amini wapumbavu? Hakika wao ndio wapumbavu, lakini hawajui tu.¹³

14. Na wanapo kutana na walio amini husema: Tumeamini. Na wanapo kuwa peke yao na mashet'ani wao husema: Hakika sisi tu pamoja nanyi. Hakika sisi tunawadhikiki tu.¹⁴

15. Mwenyezi Mungu atawadhikiki wao na atawawacha katika upotofu wao wakitangatangata ovyo.¹⁵

16. Hao ndio walio nunua upotofu kwa uwongofu; lakini biashara yao haikupata tija, wala hawakuwa wenye kuongoka.¹⁶

17. Mfano wao ni kama mfano wa aliye koka moto, na ulipo tanda mwangaza wake kote kote Mwenyezi Mungu aliiondoa nuru yao na akawawacha katika giza, hawaoni.¹⁷

18. Viziwi, mabubu, vipofu; kwa hivyo hawatarejea.¹⁸

19. Au ni kama mvua kubwa itokayo mbinguni, ina giza na radi na umeme; wakawa wakitia vidole vyao masikioni mwao kwa ajili ya mingurumo, kwa kuogopa kufa. Na Mwenyezi Mungu amewazunguka makafiri.¹⁹

20. Unakaribia umeme kunyakua macho yao. Kila ukiwatolea mwangaza huenda, na unapo wafanyia giza husimama. Na angelitaka Mwenyezi Mungu angeliondoa kusikia

13 Akitokea mtu kuwanasihani na kuwaongoza kwa kuwaambia: "Kubalini yalio waajibu." Nako ni kuwa muamini Imani safi kama wanavyo amini watu wakamilifu wanao itikia wito wa akili, wao hufanya maskhara na kejeli na husema: "Si laiki yetu sisi kuwafuata hawa wajinga, wapungufu wa akili." Mwenyezi Mungu anawarudi kwa ule ubishi wao na kuwahukumia kuwa ni wao tu ndio wajinga, wapumbavu, lakini wao hawajui kwa ujuzi wa yakini kuwa ujinga na kukosa kuelewa ni kwao wao tu.

14 Hawa wanaafiki wakiwakuta Waumini wa kweli husema: "Sisi tunaamini hayo hayo mnayo amini nyinyi," yaani kumkubali Mtume na wito wake, "na sisi tu pamoja nanyi katika itikadi." Wakisha ondoka wakakutana na wenzao wanao shabihiana na mashetani kwa fitina na ufisadi, huwaambia: "Sisi tu pamoja nanyi katika njia yenu na kazi yenu, lakini tukiwaambia yale hao Waumini kwa ajili ya kuwalazia na kuwadhihiki tu."

15 Mwenyezi Mungu *Subhana* atawalipa kwa huko kudhihiki kwao, na atawaandikia uangamifu unao lingana na hayo maskhara yao na dharau zao. Atawatendea inavyo stahili kutendewa mwenye kudhihiki, na anawapa muhula tu katika dhulma yao iliyo ovu, inayo watia upofu wasiione haki. Kisha khatimaye ndipo atapo watia mkononi kwa adhabu yake.

16 Na hawa (wanaafiki) kwa kukhiari upotofu badala ya uwongofu wamekuwa kama mfanya biashara aliye khiari kwa biashara yake bidhaa mbovu ya kuchina, basi hafanikiwi kupata faida yoyote. Hupoteza rasilmali yake. Na wao basi hawaongokewi katika 'amali yao.

17 Hali ya watu hawa katika unaafiki wao ni kama hali ya mwenye kuwasha moto apate nafuu yeye na watu wake. Moto ukisha waka ukatoa mwangaza kunawiri kote, Mwenyezi Mungu huwaondolea nuru wenye kuwasha wakawa katika giza zito, hawaoni chochote. Kwa sababu Mwenyezi Mungu aliwatunukia sababu za kuongoka, nao hawakuzishika. Kwa hivyo macho yao yakazibwa, wakastahiki kubaki katika kuemewa na upotovu.

18 Watu hawa ni kama viziwi, kwani wamepoteza manufaa ya kusikia; hawaisikii Haki kwa msikio wa kuikubali na kuitikia. Nao ni kama bubu, kwa sababu hawatamki la uwongofu au la Haki. Na wao kama vipofu, kwani hawanufaiki kwa macho yao. Hawazingatii na kujikataza. Basi hao hawaachi upotovu wao.

19 Au mfano wa hali yao katika kubabaika kwao, na hadi ya mambo yanavyo waemea, na kutokufahamu nini liwafaalo na nini linalo wadhuru, ni kama hali ya watu walio teremkiwa na mvua kutoka mbinguni, yenye radi na mingurumo, wanatia ncha za vidole vyao masikioni mwao ili ati wasisikie sauti za mingurumo, na huku wanaogopa kufa, wakidhani kuwa kule kujiziba kwa vidole kutawalinda na mauti. Watu hao ikiteremka Qur'ani - na ndani yake ikabainisha giza la ukafiri na ikatoa maonyo ya juu yake, na ikabainisha Imani na mwangaza wake unao meremeta, na yakabainishwa mahadharisho na namna mbali mbali za adhabu - wao hujitenga nayo na wakajaribu kuepukana nayo kwa kudai kuwa ati kwa kujitenga nayo wataepukana na adhabu. Lakini Mwenyezi Mungu amewazunguka makafiri kila upande kwa ujuzi wake na uwezo wake.

kwao na kuona kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.²⁰

21. Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka.²¹

22. (Mwenyezi Mungu) ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa kama tandiko, na mbingu kama paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni, na kwayo akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua.²²

23. Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyo mteremshia mja wetu basi leteni sura moja ya mfano wake, na muwaite mashahidi wenu badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli.²³

24. Na mkitofanya - na wala hamtofanya kamwe - basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe walio andaliwa hao wanao kanusha.²⁴

25. Na wabashirie walio amini na wakatenda mema kwamba watapata mabustani yapitayo mito kati yake; kila watapo pewa matunda humo, watasema: Haya ndiyo kama tuliyo pewa mbele. Na wataletewa matunda yaliyo fanana; na humo watakuwa na wake walio takasika; na wao humo watadumu.²⁵

20 Huu umeme mkali wa kuonya unakaribia kunyakua macho yao kwa ukali wake, nao kwa hakika unawamurikia njia kidogo wapate kwenda khatua chache kwa mwangaza wake, na unapo katika umeme kiza kinazidi, basi wao husimama hawajui watendeje, wamepotea. Basi hawa wanaafiki dalili na ishara zinapo watolea mwangaza huwa na hamu ya kutaka kuongoka, lakini mara punde hurejea kule kule kwenye ukafiri na unaafiki.

Mwenyezi Mungu, Mkunjufu wa uwezo akitaka kitu hukitenda tu, haemewi na chochote katika ardhi wala katika mbingu.

21 Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuanzeni, akakuumbeni akakuleeni, kama alivyo waumba walio kutangulieni. Kwani Yeye ndiye Muumba wa kila kitu. Haya ni hivyo ili mpate kuzitayarisha nafsi zenu, na mzitengeneze kwa ajili ya utukufu wa Mwenyezi Mungu na uangalizi wake. Kwa hivyo nafsi zenu zitahirike na zipate kuifuata Haki, na ziogope mwisho muovu.

22 Ni Yeye Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye itandika ardhi kwa kudra yake, na akaikunjua ili isahilike kwenu kuweza kuikalia na kunafiika kwayo. Akajaalia juu yenu mbingu zililo nyanyuka na sayari zake mfano wa jengo lililo jengwa vilivyo, na akakuleteeni njia za uhai na neema - nayo ni maji - aliyo yateremsha kutoka mbinguni, akayafanya ndiyo sababu ya kutoa mimea na miti ya matunda ambayo amekuruzukuni faida yake. Basi haifai baada ya haya mkawaza kuwa Mwenyezi Mungu ana washirika mkawaabudu kama kumuabudu Yeye, kwani Yeye hana mfano wake wala mshirika. Na nyinyi kwa maumbile yenu mnajua kwa yakini kuwa Yeye hana mfano wala mshirika. Basi msiyaharibu maumbile haya. (*Tazama* Maelezo 2:22)

23 Na ikiwa mna shaka kuisadiki hii Qur'ani tunayo mteremshia mja wetu Muhammad, basi mnayo hoja iliyo dhaahiri itayo kubainishieni haki: jaribuni kuleta kama hizi za Qur'ani katika ufasihi wake, na hukumu zake, na ilimu zake, na uwongofu wake wote, na muwaite watakao shuhudia kwamba mmeleta mfano wake, mtake msaada kwao, na wala hamtowapata. Na mashahidi hao ni mbali na Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu anamuunga mkono mja wake kwa hichi Kitabu chake, na anamshuhudia kwa vitendo vyake. Haya ikiwa ni kweli nyinyi mnaitilia shaka hii Qur'ani.

24 Basi ikiwa hamtoweza kuleta moja mfano wa hizi za Qur'ani - na kabisa hamtoweza kwa njia yoyote, kwani viumbe hawawezi hayo kwa kuwa Qura'ani ni maneno ya Muumba - basi waajibu wenu mziepuke sababu zitazo kuleteeni adhabu ya akhera, nayo ni Moto ambao utakuwa kuni zake za kuwashia ni hao makafiri na masanamu yao. Moto huu umetengenezwa kwa ajili ya kuwaadhibu wapinzani wenye inda.

25 Ikiwa hizi ni adhabu za waovu wapinzani, basi Pepo ndio makao ya Waumini. Waambie wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Kitabu chake, na wakaikubali haki bila ya kutia shaka au wasiwasi, na wakatenda vitendo vyema - waambie khabari ya kuwafurahisha na kukunjua vifua vyao; nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu amewaandalia mabustani yenye mazao, yapitayo mito chini ya miti yake na majumba yake. Kila Mwenyezi Mungu akiwaruzuku matunda ya hizo bustani wao husema: "Haya yamefanana na yale tuliyo pewa kabla." Kwani matunda haya yanashabihiana kwa , lakini

26. Hakika Mwenyezi Mungu haoni haya kutoa mfano hata wa mbu na ulio wa zaidi yake. Ama wale walio amini hujua ya kwamba hiyo ni haki iliyo toka kwa Mola wao Mlezi, lakini wale walio kufuru husema: Ni nini analo kusudia Mwenyezi Mungu kwa mfano huu? Kwa mfano huu huwapoteza wengi na huwaongoa wengi; lakini hawapotezi ila wale wapotovu,²⁶

27. Wanao vunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kwisha ifunga, na wakayakata aliyo amrisha Mwenyezi Mungu kuungwa, na wakafanya uharibifu katika nchi; hao ndio wenye khasara.²⁷

28. Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu na hali mlikuwa wafu akakufufueni! Kisha atakufisheni, tena atakufufueni, kisha kwake mtarejeshwa?²⁸

29. Yeye ndiye aliye kuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi. Tena akazielekea mbingu, na akazifanya mbingu saba. Naye ndiye Mjuzi wa kila kitu.²⁹

30. Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka humo atakaye fanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyo yajua.³⁰

yanakhitalifiana kwa utamu na ladha. Na watakuwa nao humo pia wake walio kamilika walio safi, wasio kuwa na ila yoyote. Na katika Pepo hii wataishi maisha ya milele wala hawatotoka humo.

26 Mwenyezi Mungu huwaletea mifano watu kueleza hakika ya mambo yalivyo juu, kwa kufananisha na vidudu vidogo na pia vitu vikubwa. Wasio amini waliikejeli hiyo mifano ya vijidudu vidogo kama nzi na buibui. Basi Mwenyezi Mungu aliye takasika haoni aibu kama wanavyo aibika watu kwa kuona haya. Hana la kumzuia asiwape waja wake mfano wowote autakao hata ukiwa mdogo vipi. Kwa hivyo ni sawa kabisa kupiga mfano wa mbu na kilio zaidi kuliko hivyo. Na walio amini wanajua kuwa hii ni mifano, na kuwa huu ni ukweli utokao kwa Mwenyezi Mungu. Ama walio kufuru hawapendi hayo, na husema: “Mwenyezi Mungu anataka nini kwa mfano huu?” Na mfano kama huu huwa ni sababu ya kupotea wale wasio tafuta haki wala hawaitaki, na huwa ni sababu ya kuwaongoa wenye kuamini na kuitaka haki. Basi hawapotei ila waasi walio kwisha potea.

27 Na hao walio kwisha potea ni wale ambao wanaivunja ahadi ya Mwenyezi Mungu, na wao ndio wasio ishika vilivyo ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyo iweka katika nafsi zao tangu kuumbwa, kuwa ni fungamano la akili yenye kutambua na yenye kuunga mkono Utume, na wakayakata yale aliyo yaamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, kama vile kuwaangalia jamaa, na kupendana na kutendana mema, na kuoneana hurumu watu kwa watu; na wakafanya fisadi katika nchi kwa mambo maovu na kuzua fitna na kuchochea vita na kuharibu majenzi. Hao ndio wenye kuleta khasara kwa kufisidi khulka yao walio umbwa nayo, na wakawagawa watu mapande mapande, badala ya kuleta mapenzi na kuoneana huruma kama inavyo stahiki. Kwa vitendo vyao hivyo watapata hizaya duniani na adhabu huko Akhera.

28 Hakika hali yenu instaaajabisha! Vipi mnakufuru na wala hapana sababu yoyote ya kutegemewa katika kukufuru kwenu? Ukiangalia hali yenu utaona inakataa ukafiri huu wala hamna udhuru wowote. Kwani nyinyi mlikuwa maiti, hamna uhai, akakuumbeni Mwenyezi Mungu na akakupeni uhai na umbo zuri. Kisha ni Yeye atakaye kurejezeni muwe maiti baada ya kutimia wakati wenu. Kisha atakufufueni muwe hai mara nyingine kwa ajili ya hisabu na malipo. Kisha mtarejea kwake, wala hamwendi kwa mwenginewe, mtarejea, kwa ajili ya hisabu na malipwa kwa vitendo vyenu.

29 Mwenyezi Mungu anaye pasa kuabudiwa na kut’iua ndiye aliye kufadhilini. Akaumba kwa ajili ya manufaa na faida yenu kila neema inayo patikana duniani, kisha baadae akazielekea mbingu akaziumba mbingu saba kwa mpango. Katika hayo yapo mnayo yaona na msiyo yaona. Na Mwenyezi Mungu amevizunguka vitu vyote, na anavijua vyote.

30 Mwenyezi Mungu, *Subhanahu*, Aliye Takasika, amebainisha kuwa ni Yeye ndiye aliyempa uhai mtu, na akamweka duniani. Kisha amebainisha vile vile asli ya kumweka mwanaadamu na ujuzi aliyo mpa, na akakumbushwa hayo. Basi kumbuka, ewe Muhammad, neema nyingine ya Mola wako Mlezi kumpa mtu, nayo ni pale alipo waambia Malaika: Mimi nitajaalia awepo katika ardhi mfwatizi, ambaye nitamweka hapo, na nimpe madaraka, naye ni Adam na vizazi vyake. Mwenyezi Mungu atamweka kama Khalifa, au naibu wa kuimarisha dunia, na kutekeleza amri, na kuzitengeneza nafsi. Malaika wakauliza kutaka kujua

31. Na akamfundisha Adam majina ya vitu vyote, kisha akaviweka mbele ya Malaika, na akasema: Niambieni majina ya hivi ikiwa mnasema kweli.³¹
32. Wakasema: *Subhanaka*, Wewe umetakasika! Hatuna ujuzi isipokuwa kwa uliyo tufunza Wewe. Hakika Wewe ndiye Mjuzi Mwenye hikima.³²
33. Akasema: Ewe Adam! Waambie majina yake. Basi alipo waambia majina yake alisema: Sikukwambieni kwamba Mimi ninajua siri za mbinguni na za duniani, na ninayajua mnayo yadhahirisha na mliyo kuwa mnayaficha?³³
34. Na tulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam, wakamsujudia wote isipo kuwa Iblis, alikataa na akajivuna na akawa katika makafiri.³⁴
35. Na tulisema: Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani, na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, lakini msiukaribie mti huu tu; mkawa katika wale walio dhulumu.³⁵
36. Lakini Shet'ani aliwateleza hao wawili na akawatoa katika waliyo kuwamo, na tukasema: Shukeni, nanyi ni maadui nyinyi kwa nyinyi. Katika ardhi yatakuwa makaazi yenu na starehe kwa muda.³⁶
37. Kisha Adam akapokea maneno kwa Mola wake Mlezi, na Mola wake Mlezi alimkubalia toba yake; hakika Yeye ndiye Mwingi wa kukubali toba na Mwenye kurehemu.³⁷

nini siri ya hayo, wakasema: Je, utaweka katika ardhi atakaye leta uharibifu humo kwa maasi, na atakaye mwaga damu kwa uadui na mauwaji kwa kufuata tabia yake ya matamano, na ilhali sisi tunakutakasa na yasiyo laiki na utukufu wako, na tunasafisha kumbusho lako, na tunakutukuza? Mola wao Mlezi akajibu: Mimi ninajua maslaha ya hayo msiyo yajua nyinyi.

31 Na baada ya Mwenyezi Mungu kwisha kumuumba Adam na akamfundisha majina ya vitu vyote na sifa zao ili atue katika ardhi na anufaika navyo, aliwaletea hivyo vitu Malaika na akawaambia: Niambieni majina ya vitu hivi na sifa zao kama kweli nyinyi ndivyo kama mnavyo dhani kuwa mnastahiki kupewa madaraka katika ardhi, na kuwa hapana aliye bora kuliko nyinyi kwa sababu ya ut'iifu wenu na ibada zenu.

32 Malaika wakatambua upungufu wao, wakasema: Sisi tunakutakasa Ewe Mola wetu Mlezi kwa mtakaso ulio laiki nawe. Tunakiri kuwa tumeshindwa, na hatuwezi kupinga. Kwani hatuna ilimu kuliko uliyotupa Wewe, na Wewe ndiye Mjuzi wa kila kitu, na Mwenye hikima na hukumu katika kila jambo ulitendalo.

33 Mwenyezi Mungu alimwambia Adam: Watajia Malaika khabari za vitu hivi. Akataja; na ukadhiri ubora wake juu yao. Na hapo Mwenyezi Mungu akawaambia kuwakumbusha vipi ujuzi wake ulivyo enea: Sikukwambieni kuwa Mimi ninajua siri za mbingu na ardhi, na hapana ajuae hayo isipo kuwa Mimi, na Mimi ninajua mnayo yadhahirisha katika kauli yenu, na mnayo yaficha katika nafsi zenu.

34 Na kumbuka Ewe Nabii! Tulipo waambia Malaika: Mnyenyekeeni Adamu kwa kumwamkia na kuukiri ubora wake. Wakat'ii Malaika wote ila Iblis. Yeye alikataa kusujudu akawa miongoni mwa walio asi, walio zikataa neema za Mwenyezi Mungu, na hikima yake, na ujuzi wake.

35 Kisha Mwenyezi Mungu alimuumba Adam na mkewe, na akawaamrisha wakae katika Bustani ya neema. Akamwambia: Kaa wewe na mkeo katika Bustani hii na kuleni humo mtakavyo vya kutosha bila ya kutaabika, na kaeni mtakapo, mle mtakacho. Lakini Mwenyezi Mungu aliwatajia mti maalumu na akawahadharisha wasiule, na akawaambia: Msiukaribie mti huu, wala msile matunda yake. Mkifanya hivyo mtakuwa miongoni mwa walio dhulumu, na mtakuwa waasi.

36 Lakini Iblis, anaye mhusudu na kumchukia Adam, alimfanyia vitimbi, akawadanganya mpaka wakateleza wakala mti walio katazwa. Mwenyezi Mungu akawatoa katika ile neema na ukarimu walio kuwa nayo. Mwenyezi Mungu Mtukufu akawaamrisha washukie kwenye ardhi waishi humo wao na vizazi vyao, na wawe na uadui baina yao kwa wao kwa sababu ya ushindani na kupotozwa na Shetani. Na huko kwenye ardhi pawe pahali pa kukaa kwao na kupata maisha, na kustarehe kutako kwisha kwa kutimia wakati.

37 Adam na mkewe walitambua makosa yao na kujidhulumu nafsi zao. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimfunza Adam baadhi ya maneno ya kutubia na kuomba msamaha na akayasema. Mwenyezi Mungu alimkubalia toba yake, na akamsamehe, kwani Yeye ni mwingi wa kukubali toba, naye ni Mwenye

38. Tukasema: Shukeni nyote; na kama ukikufikieni uwongofu utokao kwangu, basi watakao fuata uwongofu wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.³⁸
39. Na wenye kukufuru na kuzikanusha ishara zetu, hao ndio watakao kuwa watu wa Motoni, humo watadumu.³⁹
40. Enyi Wana wa Israili! Kumbukeni neema yangu niliyo kuneemesheni, na timizeni ahadi yangu, na Mimi nitatimiza ahadi yenu, na niogopeni Mimi tu.⁴⁰
41. Na aminini niliyo yateremsha ambayo yanasadikisha mliyo nayo, wala msiwe wa kwanza kuyakataa. Wala msiuze Ishara zangu kwa thamani ndogo. Na niogopeni Mimi tu.⁴¹
42. Wala msichanganye kweli na uwongo na mkaificha kweli nanyi mnajua.⁴²
43. Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na inameni pamoja na wanao inama.⁴³
44. Je! Mnawaamrisha watu mema na mnajisahau nafsi zenu, na hali nyinyi mnasoma Kitabu? Basi je, hamzingatii?⁴⁴
45. Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu,⁴⁵
46. Ambao wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao Mlezi na ya kuwa hakika watarejea kwake.⁴⁶

kuwarehemu waja wake wanyonge.

38 Tukamwambia Adam na mkewe na vizazi vyao vijavyo na Iblis: Shukeni katika ardhi, na huko mtalazimishwa mambo. Yakikujieni hayo kutokana na Mimi - na hapana shaka yatakujieni - basi wale watakao itikia amri yangu, na wakafuata uwongofu wangu hawataona khofu yoyote, na hawatopata huzuni, kwa kukosa thawabu, kwa sababu Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa atendaye mema.

39 Na wale ambao watapinga na watawakanusha Mitume wa Mwenyezi Mungu na Vitabu vyake, hao ni watu wa Motoni, watabaki huko milele, wala hawatatoka wala hawatakufa.

40 Enyi Wana wa Israili kumbukeni neema zangu nilizo kutunuki ni nyinyi na wazee wenu kwa kuzifikiri na kushukuru na kutimiza agano langu nililo lichukua kwenu, na nyinyi nafsi zenu mkalikiri, nalo ni Imani, na Vitendo vyema, na kuwasadiki Manabii wajao baada ya Musa, ili Nami nitimize ahadi yangu kwenu, nayo ni kukulipeni malipo mema, na neema ya kudumu. Na wala msimwogope mtu yeyote isipo kuwa Mimi, na tahadharini na kufanya mambo yatakayo nifanya nikasirike nanyi. (*Tazama Maelezo 2:40*)

41 Na isadikini Qur'ani iliyo teremshwa kusadikisha vile vitabu mliyavyo navyo, na kufunza Tawhidi (kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja) na kumwabudu Mwenyezi Mungu, na uadilifu baina ya watu. Wala msikimbilie kutaka kuipinga Qur'ani msije mkawa ndio wa mwanzo kuikanya, na ilhali ifaavyo nyinyi ndio muwe wa mwanzo kuiamini. Wala msiziache Ishara za Mwenyezi Mungu mkenda badala yake mkachukua chenginecho kipitacho njia katika starehe za uhai wa dunia. Na niogopeni Mimi tu, na fuateni Njia yangu, na wacheni upotovu.

42 Wala msichanganye Haki iliyo toka kwangu na upotovu mlio uzua nyinyi, hata ikawa halijulikani la kweli na la uwongo. Wala msii fiche Haki, na katika hiyo Haki ni kumsadiki Muhammad, na nyinyi mnajua kuwa yeye ni wa kweli na wa kusadikiwa.

43 Itikieni Imani. Shikeni Sala yenye nguzo zilizo simama baraabara. Na toeni Zaka muwape wanao stahiki. Na salini pamoja na jamaa wa Kiislamu ili mpate malipo ya Sala na thawabu za kusali jamaa. Na haya yanalazimu kuwa muwe Waislamu.

44 Je, mnawataka watu wafanye kheri, na wajilazimishe ut'iifu, na waache maasia, kisha nyinyi hamtendi myasemayo, wala hamjilazimishi nafsi zenu kwa yale myatakayo? Kwa hivi mnajipoteza nafsi zenu, kama kwamba mmezisahau, na ilhali nyinyi mnasoma Taurati na ndani yake pana maonyo na mikemeo kwa mwenye kusema asilo litenda. Basi nyinyi hamna akili ya kukuzuieni na kwenda mwendo huu wa kutukanisha?

45 Na tafuteni msaada wa kutekeleza waajibu kwa subira na kuizuia nafsi isitende yanayo udhi. Katika hayo ni kwa kufunga Saumu, na kwa Sala ambalo ni jambo kubwa lenye kuusafisha moyo na kuzuia kutenda machafu na maovu, na kwa hivyo ndio yakawa mazito ila kwa wenye kupenda ut'iifu ambao nyoyo zao zimetulia kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu.

46 Hao ndio wanyenyekevu walio tulia nyoyo zao, ambao wanaiamini Siku ya mwisho, na wana yakini

47. Enyi Wana wa Israili! Kumbukeni zile neema zangu nilizo kuneemesheni, na nikakuteuweni kuliko wote wengineo.⁴⁷
48. Na iogopeni Siku ambayo mtu hatomfaa mtu kwa lolote, wala hayatakubaliwa kwake maombezi, wala hakitapokewa kikomboleo kwake; wala hawatanusuriwa.⁴⁸
49. Na vile tulipo kuokoeni kwa watu wa Firauni walio kupeni adhabu mbaya, wakiwachinja wana wenu wa kiume na wakawawacha hai wanawake; na katika hayo ulikuwa ni mtihani mkubwa ulio toka kwa Mola wenu Mlezi.⁴⁹
50. Na tulipo ipasua bahari kwa ajili yenu na tukakuokoeni, tukawazamisha watu wa Firauni, na huku mnatazama.⁵⁰
51. Na tulipo muahidi Musa masiku arubaini, kisha mkachukua ndama (mkamuabudu) baada yake, na mkawa wenye kudhulumu.⁵¹
52. Kisha tukakusameheni baada ya hayo, ili mpate kushukuru.⁵²
53. Na tulipo mpa Musa Kitabu na pambanuo ili mpate kuongoka.⁵³
54. Na Musa alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmezidhulumu nafsi zenu kwa kuchukua kwenu ndama (kumuabudu). Basi tubuni kwa Muumba wenu na ziueni nafsi zenu. Haya ni bora kwenu mbele ya Muumba wenu. Naye akapokea toba yenu. Hakika Yeye ndiye apokeaye toba na Mwenye kurehemu.⁵⁴

kuwa watakutana na Mola wao Mlezi wakati wa kufufuliwa, na kwake Yeye pekee ndio watarejea ili awahisabie kwa yale waliyo yatenda na awalipe kwayo.

47 Enyi Wana wa Israili! Kumbukeni neema zangu nilizo kuneemesheni kwa kukutoeni katika dhulma ya Firauni, na nikakuongoeni na nikakuwekeni imara katika nchi baada ya kuwa mlikuwa mkionewa humo. Mshukuruni kwa kumt'ii Mwenye kukutunukieni hayo. Na kumbukeni kuwa Mimi niliwapa baba zenu mlio zalikana kutoka kwao nisiyo wapa wowote wengineo wakati wenu. Haya wanaambiwa taifa la Mayahudi walio kuwako zama za Mtume.

48 Iogopeni Siku ya Hisabu kali, Siku ya Kiyama, siku ambayo hapana mtu ataeweza kumtetea mtu, na wala hapana mtu ataye mfaa mtu, wala hakubaliwi mtu kuleta mwombezi, kama ilivyokuwa hatokubaliwa mtu kutoa fidia ya dhambi, wala hapana mtu ataye weza kuizuia adhabu isimpate mwenye kustahiki.

49 Na kumbukeni katika neema zetu juu yenu kuwa tumekuokoeni kutokana na mateso ya Firauni na wasaidizi wake walio kuwa wakikuonjesheni adhabu kali kabisa, kwa kuwa wakiwachinja wana wenu wanaume - kwa khofu kuwa miongoni mwao atatokea wa kupindua utawala wa Firauni - na wakiwabakisha wanawake ili wawafanye wajakazi wao wa kuwatuma. Na katika adhabu hizi na uteketezaji huu wa umma ni majaribio makuu kutokana kwa Mola wenu, na ni mtihani mkuu kwenu.

50 Kumbukeni vile vile katika neema alizo kuneemesheni Mwenyezi Mungu pale tulipo kupasulieni bahari - na tukayagawa maji katikati ili mpate kupita - mkaokoka, Firauni na askari wake wasikupateni. Na kwa fadhila yetu mkavuka na tukawapatiliza adui zenu kwa sababu yenu, tukawazamisha mbele ya macho yenu. Nyinyi mkawa mnawaona wanazama, na bahari ikiwafunika baada ya nyinyi kwisha vuka salama.

51 Na kumbukeni wakati Mola wenu alipo agana na Musa muda wa masiku arubaini kwa ajili ya mazungumzo. Alipo kwenda walipo agana na akarejea alikukuteni mmekwisha geuka, na mkamfanya ndama aliye muunda Saamiriyu ndiye wa kuabudiwa. Mkawa kwa hivyo ni wenye kudhulumu kwa kumfanyia Mwenyezi Mungu aliye kuumbeni na kukuokoeni ana mshirika wake. (Tazama Maelezo 2:51)

52 Kisha tukakusameheni na tukaifuta adhabu yenu mlipo tubu na mkapata msamaha kwa dhambi zenu, ili mpate kumshukuru Mola Mlezi wenu kwa huko kufuta kwake makosa yenu, na kusamehe kwake, na fadhila zake.

53 Na kumbukeni tulipo kuneemesheni kwa kukumteremshia Nabii wenu Musa Kitabu chetu Taurati, Kitabu ambacho kinafarikisha baina ya Haki na baat'ili, na kinabainisha baina ya Halali na Haramu, ili mpate kupata uwongozi kwa nuru yake na muongoke kutokana na upotovu kwa kuzingatia yaliyomo ndani yake.

54 Ikumbukeni siku alipo kwambieni Mtume wenu Musa: Enyi watu wangu! Mmejidhulumu kwa kumchukua ndama wa Saamiriyu mkamuabudu. Basi tubuni kwa Mola wenu aliye kuumbeni kabla

55. Na mlipo sema: Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumwone Mwenyezi Mungu waziwazi. Ikakunyakueni radi nanyi mnaangalia.⁵⁵
56. Kisha tukakufufueni baada ya kufa kwenu, ili mpate kushukuru.⁵⁶
57. Na tukakutilieni kivuli kwa mawingu na tukakuteremshieni Manna na Salwa; tukakwambieni: Kuleni vitu vizuri hivi tulivyo kuruzukuni. Nao hawakutudhulumu Sisi lakini walikuwa wanajidhulumu nafsi zao.⁵⁷
58. Na tulipo sema: Ingieni mji huu, na humo mle mpendapo maridhawa, na ingieni katika mlango wake kwa unyenyekevu, na semeni: Tusamehe! Tutakusameheni makosa yenu, na tutawazidishia wema wafanyao wema.⁵⁸
59. Lakini walio dhulumu waliabadili kauli isiyo kuwa waliyo ambiwa. Kwa hivyo tukaiteremsha juu ya wale walio dhulumu adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya walivyo kuwa wamepotoka.⁵⁹
60. Na Musa alipo omba maji kwa ajili ya watu wake, tulimwambia: Lipige jiwe kwa fimbo yako. Mara zikatimbuka chemchem kumi na mbili; kila kabila ikajua mahali pake pa kunywa. Tukawaambia: Kuleni na mnywe riziki ya Mwenyezi Mungu, wala msiasi katika nchi mkafanya uharibifu.⁶⁰
61. Na mlipo sema: Ewe Musa! Hatuwezi kuvumilia chakula cha namna moja tu,

hamjawa kitu, kwa kuzighadhibikia nafsi zenu ovu zenye kuamrisha maovu, na zifanyeni hizo nafsi ziwe nyonge, ili mpate nafsi mpya zililo safi. Mwenyezi Mungu alikusaidieni kwa hayo na akakuwezesheni mkaweza, na hiyo ni kheri itokayo kwa Muumba wenu. Na haya ni kabla ya kutubu kwenu, Naye akakusameheni. Kwani Yeye ni mwingi wa kukubali toba kwa waja wake, na mwingi wa kuwarehemu.

55 Na kumbukeni kauli yenu mlio mwambia Musa: Kwamba sisi hatukukubali wewe mpaka tumwone Mwenyezi Mungu waziwazi hivi hivi kwa macho bila ya kificho. Ikakuchukueni radi na moto kutoka mbinguni, ikakutikiseni kuwa ni malipo ya inadi yenu na dhulma zenu, na kutaka kwenu jambo ambalo ni muhali kutokea kwenu. Nanyi mnaiona hali yenu na balaa na adhabu zilizo kusibuni kwa mpigo wa radi hiyo.

56 Kisha tukakuzindueni kutokana na huko kudawaa kwenu na kupwelewa, na tukakufundisheni ili mpate kuishukuru neema yetu kwa hayo, na mpate kuiunga mkono Haki ya Mwenyezi Mungu kwa kupitia njia ya shukrani hii.

57 Na katika fadhila zetu juu yenu ni kuwa tumekuleteeni mawingu yawe kama ni kivuli kukulindeni na mwako wa jua kali, na tukakuteremshieni Manna, nacho ni kitu kitamu kama asali kinaanguka juu ya miti linapo chomozia jua. Kadhaalika tumekuteremshieni Salwa, naye ni ndege aliye nona, nao wakikujieni kwa makundi asubuhi na jioni ili mle mstarehe. Na tukakwambieni: Kuleni vilivyo vyema katika riziki yetu. Hawa watu wakaikufuru neema. Na haya hayakutudhuru Sisi, lakini wamejidhulumu nafsi zao. Kwani madhara ya uasi unawarejea wao watendao. (*Tazama Maelezo 2:57*)

58 Na kumbukeni enyi Wana wa Israili! Tulipo kwambieni: Ingieni katika mji mkubwa aliyo kutajieni Nabii wenu Musa na mle katika viliomo humo kama mnacho kitaka, kwa wingi na kwa wasaa, kwa sharti lakini kuwe kuingia kwenu kwa upole na unyenyekevu, kupitia mlango aliyo utaja Nabii wenu. Na kwamba hapo mumuombe Mwenyezi Mungu akusameheni makosa yenu. Kwani mwenye kufanya hayo kwa ikhlasi, usafi wa niya, tunamfutia makosa yake. Na mwenye kuwa mtenda mema aliye mt'ifu tunamzidishia thawabu na ukarimu juu ya kumsamehe na kumfutia dhambi.

59 Lakini walio dhulumu walikwenda kinyume na amri za Mola wao Mlezi, wakasema sio walio amrisha wayaseme, kwa kudhihaki na kuasi. Basi jaza yao ni kuwa Mwenyezi Mungu aliwateremshia juu yao adhabu kuwa ndiyo malipo ya ukosefu wao na kuzivunja amri za Mola wao Mlezi.

60 Na kumbukeni, enyi Wana wa Israili, siku Nabii wenu Musa alipo taka maji kutokana na Mola wake Mlezi kiliposhitadi kiu jangwani, Nasi tukakurehemuni. Tukamwambia Musa: Lipige jiwe kwa fimbo yako, yakatimbuka maji kutoka chemchem kumi na mbili. Kila kikundi na chemchem yake, na walikuwa makundi thinaashara. Basi kila kabila ikawa na pahala pake pa kunywa. Na tukakwambieni: Kuleni Manna na Salwa, na kunyweni maji haya yanayo timbuka, na muwache mlio nayo, wala msipite mipaka kwa uharibifu katika nchi, bali wacheni maasia.

basi tuombe kwa Mola wako Mlezi atutolee vile vinavyo mea katika ardhi, kama mboga zake, na matango yake, na thom zake, na adesi zake, na vitunguu vyake. Akasema: Mnabadili kilicho duni kwa kilicho bora? Shukeni mjini, huko mtapata mlivyo viomba. Na wakapigwa na unyonge, na umasikini, na wakastahili ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na haya ni kwa sababu walikuwa wakiyakataa maneno ya Mwenyezi Mungu, na wakiwauwa Manabii pasipo haki. Hayo ni kwa walivyo asi na wakapindukia mipaka.⁶¹

62. Hakika Walio amini, na Mayahudi na Wakristo, na Wasabai; yeyote atakaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na akatenda mema basi watapata malipwa yao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.⁶²

63. Na tulipo chukua ahadi yenu, na tukaunyanyua mlima juu yenu (tukakwambieni): Shikeni kwa nguvu haya tuliyo kupeni, na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kujilinda.⁶³

64. Kisha mligeuka baada ya haya. Na lau kuwa si fadhila za Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema zake, mngeli kuwa miongoni mwa wenye kukhasirika.⁶⁴

65. Na hakika mlikwisha yajua ya wale miongoni mwenu walio ivunja Sabato, (siku ya mapumziko, Juma Mosi) na tukawaambia: Kuweni manyani wadhaliifu.⁶⁵

66. Kwa hivyo tukayafanya hayo kuwa onyo kwa wale walio kuwa katika zama zao na walio kuja baada yao, na mawaidha kwa wachamngu.⁶⁶

61 Na kumbukeni pia, enyi Mayahudi, pale wale wazee wenu walio tangulia walipo zidi jeuri zao, wasiipe neema ya Mwenyezi Mungu haki yake, wakamwambia Musa: Sisi hatutovumilia chakula hicho kwa hicho (nacho ni Manna na Salwa). Basi muombe Mola wako atutolee katika ardhi mboga, na matango, na adesi, na thom na vitunguu. Musa aliyastaajabia haya na wala hakupendezewa nayo. Akawaambia: Hivyo nyinyi mnafadhilisha vyakula namna hii kuliko vilivyo kuwa bora zaidi na vizuri zaidi, navyo ni Manna na Salwa? Basi shukeni kutoka Sinai, na ingieni katika mji mmojawapo na huko mtapata hivyo mnavyo vitaka. Na kwa sababu ya kutoridhika kwao huko na inda yao hao Mayahudi walipigwa na madhila, na ufakiri na unyonge, wakastahiki kupata ghadhabu ya Mwenyezi kwa ule mtindo wao wa inda na uasi, kukanusha ishara za Mwenyezi Mungu, na kuwauwa Manabii. Kwa haya ikawa wanaacha Haki iliyo kwisha thibiti na kukubalika. Yaliyo wapelekea hata wakaingia katika ukafiri ule na mauwaji yale ni kule kuziachia nafsi zao kupanda maasi na kufanya uadui na kupindukia mipaka katika maasia.

62 Wale walio amini, nao ni Manabii wa zamani, na Mayahudi, na Wakristo, na wanao tukuza nyota na malaika, na wanao uamini ujumbe wa Muhammad baada ya kuteuliwa kuwa ni Mtume, na wakaamini kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mmoja wa pekee, na wakaamini kuwa kupo kufufuliwa na kuhisabiwa Siku ya Kiyama, na wakatenda vitendo vyema duniani, basi watu hawa wana malipwa yao yaliyo wekwa kwa Mola wao Mlezi. Wala haitowapata khofu ya kuadhibiwa, na wala haitowafika huzuni kwa kukosa thawabu. Na Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa mwenye kutenda mema.

63 Kumbukeni pale tulipo chukua ahadi na agano juu yenu, tukaunyanyua mlima wa T'uur, tukaufanya kwa uwezo wetu kama kivuli juu yenu mpaka mkaogopa mkanyenyekea, tukakwambieni: Shikeni uwongofu na uwongozi tulio kupeni kwa nguvu na jitihadi, na mkumbuke kwa kutekeleza na kutenda yaliyo tajwa ndani ili mpate kujilinda nafsi zenu msipate adhabu.

64 Tena baada ya hayo yote mkageuka. Na lau kuwa si fadhila na rehema ya Mwenyezi Mungu juu yenu kuiakhirisha adhabu kwenu mngeli kwisha kuwa miongoni walio potea na kuangamia.

65 Na nyinyi bila ya shaka mliwajua wale walio pindukia mipaka katika siku ya Sabato, siku ya ibada na mapumziko, siku ya Juma mosi. Pale walipo kwenda kuvua samaki siku hiyo na ilhali siku hiyo ilikuwa imetengwa iwe ni siku ya mapumziko na siku kuu, na kufanya kazi siku hiyo ilikatazwa. Mwenyezi Mungu alizipotoa nyoyo za wakosefu wale, wakawa kama manyani katika pumbao lao na matamano yao. Tukawaweka mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu, wakifukuzwa kama mijibwa, watu hawataki kukaa nao, na wanawanyanyapaa kuchanganyika nao.

66 Mwenyezi Mungu ameifanya hali yao namna hii waliyo ifikia ili iwe ni kama funzo na onyo kwa wengineo, wasitende kitendo kama hichi. Ameyafanya haya ili yazingatiwe na watu wa nyakati zao

67. Na Musa alipo waambia watu wake: Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mchinje ng'ombe. Wakasema: Je! Unatufanyia mzaha? Akasema: Audhubil lahi! Najikinga kwa Mwenyezi Mungu nisiwe miongoni mwa wajinga.⁶⁷

68. Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atupambanulie ni ng'ombe gani? Akasema: Hakika Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mpevu, wala si kindi, bali ni wa katikati baina ya hao. Basi fanyeni mnavyo amrisha.⁶⁸

69. Wakasema: Tuombee kwa Mola wako atupambanulie nini rangi yake? Akasema: Yeye anasema, kuwa ng'ombe huyo ni wa manjano, na rangi yake imekoza, huwapendeza wanao mtazama.⁶⁹

70. Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atupambanulie ni yupi? Hakika tunaona ng'ombe wamefanana. Na kwa yakini, Inshaallah, Mwenyezi Mungu akipenda, tutaongoka.⁷⁰

71. Akasema: Yeye anasema: Kuwa huyo ni ng'ombe asiye tiwa kazini kulima ardhi wala kumwagia maji mimea, mzima, hana baka. Wakasema: Sasa umeleta haki. Basi wakamchinja, na walikaribia kuwa wasifanye hayo.⁷¹

72. Na mlipo muuwa mtu, kisha mkakhalifiana kwayo, na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyatoa hayo mliyo kuwa mkiyaficha.⁷²

73. Tukasema: Mpigeni kwa kipande chake (huyo ng'ombe). Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu huwahuisha wafu; na anakuonyesheni Ishara zake ili mpate kufahamu.⁷³

74. Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo, hata zikawa kama mawe au

na watakao kuja baada yao, kama tulivyo yafanya kuwa ni mawaidha kwa wale wanao mcha Mola wao Mlezi, kwani wao ndio wanao nafika kwa maonyo ya mawaidha na mazingatio.

67 Na kumbukeni pale alipo uliwa mtu na asijulikane muuwaji, Musa akawaambia watu wake: Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mchinje ng'ombe ili iwe ndio ufunguo wa kumgundua muuwaji. Lakini wakaona hayo ni mageni, baina ya yale mauwaji na kumchinja ng'ombe. Wakasema: Unatufanyia maskhara wewe Musa? Yeye akawajibu: Mimi najilinda kwa Mwenyezi Mungu asinipatimize kwa kuwa katika wajinga wanao wadhikiki waja wake.

68 Tena wakamwambia Musa wakirejea lile shauri la ng'ombe: Tutakie kwa Mola wako Mlezi atubainishie sifa za huyo ng'ombe. Akawaambia: Mwenyezi Mungu ameniambia huyo ng'ombe si mkubwa wala si mdogo, bali yu katikati baina ya upevu na uchanga. Basi hebu tekelezeni alivyo kuamrisheni Mwenyezi Mungu

69 Lakini walikakamia katika kutaradadi kwao, wakasema: Tutakie kwa Mola wako Mlezi atupambanulie nini rangi yake. Akawajibu: Mwenyezi Mungu anasema: Ng'ombe huyo ni wa rangi ya manjano iliyo koza, na safi. Ukimtazama anapendeza kwa usafi wa rangi yake ilivyo zaga.

70 Tena wakashikilia kuuliza kwao, wakasema: Tuombee kwa Mola wako Mlezi atupambanulie khasa huyo ni yupi? Kwani ng'ombe wanatudanganyikia sisi, hatujui. Na Inshallah, Mwenyezi Mungu akipenda, sisi tutaongokewa tumjue.

71 Musa akawambia: Mwenyezi Mungu anasema kuwa ng'ombe huyo bado hajatiwa kazini kwa kulima wala kumwagia maji shambani kwa ajili ya makulima. Naye hana ila yoyote, mzima kabisa, wala katika mwili wake hana kibaka chochote, wote ni wa rangi moja. Hapo tena wakamwambia: Sasa umepambanua vilivyo. Wakamtafuta ng'ombe mwenye sifa hizo wakamchinja. Na walikuwa wamekaribia wasifanye hayo kwa kukithiri masuala yao na wingi wa kushikilia kwao.

72 Na kumbukeni siku mlipo muuwa mtu, mkakhasimiana wenyewe kwa wenyewe, mkautetea ukhalifu, mkawa mkituhumiana kwa mauwaji, na hali Mwenyezi Mungu anajua hakika, na ataikashifu na kuidhihirisha juu ya kuificha kwenu.

73 Tukakwambieni kwa ulimi wa Musa: Chukueni kipande cha nyama ya huyo ng'ombe mumpige nacho, nanyi mkafanya hivyo. Mwenyezi Mungu akamfufua huyo aliye uliwa akataja jina la aliye muuwa, na kisha akafa tena. Na huo ulikuwa ni muujiza wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Musa. Kwani Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu, na kwa uwezo wake huu ndivyo anvayo huisha maiti Siku ya Kiama. Na anakuonyesheni dalili za uwezo wake ili mpate kufahamu na kuzingatia haya. (Tazama Maelezo 2:73)

ngumu zaidi; kwani kuna mawe yanayo timbuka mito, na kuna mengine yanayo pasuka yakatoka maji ndani yake, na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na mnayo yafanya.⁷⁴

75. Mnatumai watakuaminini na hali baadhi yao walikuwa wakisikia maneno ya Mwenyezi Mungu, kisha wakayabadili baada ya kuwa wameyafahamu, na hali wanajua?⁷⁵

76. Na wanapo kutana na wale walio amini husema: Tumeamini. Na wanapo kuwa peke yao, wao kwa wao, husema: Mnawaambia aliyo kufunulieni Mwenyezi Mungu ili wapate kukuhojieni mbele ya Mola wenu Mlezi? Basi hamfahamu nyinyi?⁷⁶

77. Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anayajua wanayo yaficha na wanayo yatangaza?⁷⁷

78. Na wako miongoni mwao wasio jua kusoma; hawakijui Kitabu isipo kuwa uwongo wanao utamani, nao hawana ıla ni kudhanja tu.⁷⁸

79. Basi ole wao wanao andika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu, ili wachumie kwacho pato dogo. Basi ole wao kwa yale iliyo andika mikono yao, na ole wao kwa yale wanayo yachuma.⁷⁹

80. Na walisema: Hautatugusa Moto ıla kwa siku chache tu. Sema: Mmechukua ahadi kwa Mwenyezi Mungu? Kweli Mwenyezi Mungu hatokwenda kinyume na ahadi yake. Au mnamsingizia Mwenyezi Mungu mambo msiyo yajua?⁸⁰

74 Tena nyinyi baada ya miujiza na ishara hizi zote hamkukubali wala hamkunyooka, wala nyoyo zenu hazikulainika na kunyenyekea. Bali zikawa zimekacha na ngumu, na zikabakia vile vile na ugumu wake na ushupavu wake, kama jiwe gumu katika ule ukakamavu wake, bali hizo nyoyo zenu zimeshinda jiwe kwa ugumu. Kwani yapo mawe yanayo athirika na kulainika. Yapo mawe yanayo timbuka maji yakawa mito, na yapo mawe yanayo pasuka na yakatoka maji kama chemchem, na yapo mawe kwa uwezo wa Mwenyezi yanayo nyenyekea kufuata mapenzi ya Mwenyezi Mungu yakaporomoka kutoka juu ya milima kama apendavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ama hizo nyoyo zenu,nyinyi Mayahudi, haziathiriki wala hazilainiki. Ole wenu kwa hayo! Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na vitendo vyenu, naye atakupeni adabu kwa namna mbali mbali za adhabu, ikiwa hamtoshukuru kwa neema mlizo pewa.

75 Haikufaliini enyi Waumini kutumai ya kuwa Mayahudi wataiamini Dini yenu na wakufuateni nyinyi, na ilhali katika makundi yao mbali mbali zimekusanyika sifa mbovu zinazo waweka mbali na kuiamini Haki. Walikuwapo baadhi miongoni mwao (nao ni wale Makohani) walio kuwa wakiyasikia maneno ya Mwenyezi Mungu katika Taurati, na wakiyafahamu vilivyo, kisha makusudi wakiyageuza na hali wanajua kuwa ni kweli, na kuwa vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyo teremshwa haijuzu kuvigeuza.

76 Na kilikuwapo kikundi kingine miongoni mwa wanaafiki wao wakikutana na walio amini husema kwa kuwakhadaa: Tunaamini kuwa nyinyi mnafuata Haki, na kuwa Muhammad ni Nabii aliye tajwa sifa zake katika Taurati. Na wakiwa peke yao na wenzao hulaumiana kwa kughafilika kwa baadhi yao, kwa vile ndimi zao zilivyo teleza katika kuwakhadaa Waumini kuwapa maneno ambayo yatawapa faida makhasimu zao, na wala si lazima katika udanganyifu, wakawatajia yaliyomo katika Taurati ya kueleza kwa sifa kuja kwa Muhammad na kwa hivyo itakuwa hoja juu yao Siku ya Kiyama.

77 Hivyo basi haiwapitikii watu hawa na wale kuwa Mwenyezi Mungu hana haja ya kupata hoja kama hizo? Kwani Yeye anajua wanacho kificha na wanacho kidhihirisha.

78 Na miongoni mwa Mayahudi kipo kikundi cha wajinga wasio jua kusoma, wasio jua chochote kutokana na Taurati ıla uwongo unao wafikiana na matamania yao, wanao wapachikia pachikia makohani wao, na wakaona katika mawazo yao kuwa hayo ni kweli iliyotoka Kitabuni.

79 Basi hao makohani wataangamia na watapata adhabu kwa vile wanavyo andika vitabu kwa mikono yao, kisha wakawaambia wajinga wasiojua kusoma kuwa: Hii ni Taurati iliyo toka kwa Mwenyezi Mungu. Kusudi lao ni kuwa wapate kwa hayo pato la upuuzi la kidunia, wanunue upuuzi huu kwa kuza Haki na Kweli. Basi ole wao kwa wanayo mzulia Mwenyezi Mungu, na ole wao kwa yale matunda wanayo yachuma kwa uzushi wao!

80 Na katika khitilafu zao ni haya wanayo yapata kwa makohani ya kuwa Moto hautawagusa Mayahudi

81. Naam, anaye chuma ubaya - na makosa yake yakamzunguka - hao ndio watu wa Motoni; humo watadumu.⁸¹
82. Na wale walio amini na wakatenda mema, hao ndio watu wa Peponi, humo watadumu.⁸²
83. Na tulipo funga agano na Wana wa Israili: Hamtamuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu; na muwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na semeni na watu kwa wema, na shikeni Sala, na toeni Zaka. Kisha mkageuka isipo kuwa wachache tu katika nyinyi; na nyinyi mnapuuzwa.⁸³
84. Na tulipo chukua agano lenu kuwa hamtamwaga damu zenu, wala hamtatoana majumbani mwenu; nanyi mkakubali nanyi mnashuhudia.⁸⁴
85. Kisha nyinyi kwa nyinyi mnauwana, na mnawatoa baadhi yenu majumbani kwao, mkisaidiana kwa dhambi na uadui. Na wakikujieni mateka mnawakombo, na hali kuwatoa mmekatazwa. Je! Mnaamini baadhi ya Kitabu na mnakataa baadhi yake? Basi hana malipo mwenye kutenda hayo miongoni mwenu ila hizaya katika maisha ya duniani, na Siku ya Kiyama watapelekwa kwenye adhabu kali kabisa. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na yale mnayo yatenda.⁸⁵
86. Hao ndio walio nunua uhai wa dunia kwa (uhai wa) Akhera; kwa hivyo hawatapunguziwa adhabu wala hawatanusuriwa.⁸⁶

hata wakifanya maasia namna gani ila kwa muda wa siku chache tu. Basi waambie ewe Muhammad!: Nyinyi mmeagana na Mwenyezi Mungu kwa hayo, hata mkawa mmetumaini kuwa Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake, au mnamzulia uwongo tu?

81 . Ukweli wa mambo ni kuwa nyinyi mnamzulia Mwenyezi Mungu uwongo. Kwani hukumu ya Mwenyezi Mungu inapitishwa kwa viumbe vyake vyote sawa sawa, hapana farka baina ya Yuhudi na asiye kuwa Yahudi. Wenyewe kutenda maovu, na maovu yakawazunguka hao waovu mpaka njia za kuokoka zote zikazibwa, basi hao ndio watu wa Motoni na huko watudumu milele.

82 Na wale walio amini na wakatenda mema hao ndio watu wa Peponi, kwa sababu wao wameamini na wakatimiza iliyo wajibisha Imani yao, nayo ni vitendo vyema, basi wao watakaa Peponi daima milele.

83 Mbali na haya yote, nyinyi jamaa wa Kiyahudi, mnaendelea kuyashughulikia madhambi na kuvunja ahadi, na kupindukia mipaka aliyo kuwekeeni Mwenyezi Mungu. Kumbukeni tulipo chukua ahadi kwenu katika Taurat kuwa hamtamuabudu ila Mwenyezi Mungu, na mwatendee wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na mnapo zungumza na watu mtumie maneno mazuri ya kuleta masikilizano baina yenu nao wala sio ya kukutenganisheni, na mtimize yaliyo kuwa waajibu juu yenu, nayo ni Sala, na Zaka. Na kumbukeni ulikuwaje mwendo wenu katika ahadi hiyo? Vipi mlivyo ivunja na mkajipuuzwa nao, isipo kuwa wachache tu ndio walio ifuata Haki?

84 Na kumbukeni tulipo chukua ahadi kwenu katika Taurat kuwa hamtakuwa mkimwaga damu zenu, wala hamtafukuzana katika majumba yenu. Na ahadi hiyo mnakubali kuwa ipo katika Kitabu chenu na mnashuhudia kuwa ni kweli.

85 Nanyi wenyewe kwa wenyewe mnauwana, na mnatoana majumbani, nyinyi kwa nyinyi: hawa wanawauwa hawa na hawa wanawauwa hawa; hawa wanawafukuza hawa majumbani mwao na hawa wanawafukuza hawa. Na huku mkisaidiana katika vitendo vya dhambi na uadui. Baada ya hayo wakitokea baadhi yenu wakatekwa na hao mnao shirikiana nao mnajishughulisha kwenda kuwakombo hao mateka. Mkiulizwa nini kilicho kupelekeeni kuwakombo, mnajibu kuwa vitabu vyenu vinakuamrisheni kukombo mateka wa Kiyahudi. Jee, vitabu hivyo havikukuamrisheni msimwage damu ya ndugu zenu? Havikukuamrisheni msiwatoe watu majumbani mwao? Hivyo nyinyi mnat'ii sehemu ya yaliyo kujieni katika Kitabu na mnayakataa mengineyo? Basi jaza ya mwenye kutenda hayo katika nyinyi si lolote ila kupata hizaya katika maisha ya duniani, na Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu, anaye vijua vyema vitendo vyao na siri zao, atawapeleka kwenye adhabu iliyo kali kabisa. (*Tazama* Maelezo 2:85)

86 Na hayo ni kwa kuwa wamekhiari mapato ya hii dunia ipitayo kuliko neema za Akhera zitakazo dumu. Katika haya wamekuwa kama mtu aliye uza Akhera yake kwa ajili ya kununua dunia. Basi hawatapunguziwa adhabu ya Jahannam, wala hawatapata wa kuwaokoa nayo.

87. Na hakika tulimpa Musa Kitabu na tukafuatisha baada yake Mitume wengine. Na tukampa Isa, mwana wa Mariamu, hoja zilizo waziwazi, na tukamtia nguvu kwa Roho Takatifu. Basi kila walipo kufikieni Mitume kwa yale ambayo hayapendwi na nafsi zenu, mljivuna; wengine mkawakanusha, na wengine mkawauwa.⁸⁷

88. Na walisema: Nyoyo zetu zimefunikwa. Bali Mwenyezi Mungu amewalaani kwa kufuru zao: kwa hivyo ni kidogo tu wanayo yaamini.⁸⁸

89. Na kilipo wajia Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu kinacho thibitisha waliyo nayo - na wao walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri - yalipo wajia yale waliyo kuwa wakijajua waliyakanusha. Basi laana ya Mwenyezi Mungu juu ya wakanushao!⁸⁹

90. Kiovu kweli walicho jiuza nafsi zao, nacho ni kule kukataa kwao aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya kuona maya kwa kuwa Mwenyezi Mungu humteremshia fadhila yake amtakaye miongoni mwa waja wake. Basi wamejiletea wenyewe ghadhabu juu ya ghadhabu. Na makafiri watapata mateso ya kudhalilisha.⁹⁰

91. Na wanapo ambiwa: Yaaminini aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu. Wao husema: Tunaamini tuliyo teremshiwa sisi. Na huyakataa yasiyo kuwa hayo. Na hali ya kuwa hii ndiyo Haki inayo thibitisha yale waliyo nayo wao. Sema: Mbona mliwauwa Manabii wa Mwenyezi Mungu hapo zamani ikiwa kweli mlikuwa Waumini?⁹¹

87 Enyi Mayahudi, kumbukeni vile vile, ule msimamo wenu wa upotovu na wenye dhambi kwa mnasaba wa Musa na Mitume mingine tulio watuma. Kwani tulimtumwa kwenu Musa na tukampa Taurati, na kumfwatia yeye tuliwaleta Mitume kadhaa wa kadhaa wengineo. Miongoni mwao ni: Isa bin Maryamu ambaye tulimpa miujiza na tukamuunga mkono kwa Roho Mtakatifu, naye ni Jibril Mjumbe muaminifu wa Ufunuo. Nanyi kila akikujilieni Mtume asiye wafikiana na matamano yenu mnatakabari na hamtaki kumfwata. Mitume wengine mliwakataa na kuwaambia waongo, na wengine mliwauwa khasa.

88 Hali kadhaalika msimamo wenu kwa Mtume wetu Muhammad, Nabii wa mwisho. Mlimwambia alipo kuiteni msilimu: Nyoyo zetu zimefunikwa kwa vifuniko visivyo achilia kupenya huo wito wako. Basi sisi hatuelewi kitu chochote unacho sema! Wala nyoyo zao hazikufunikwa kama wanavyo dai, lakini wamepanda kiburi tu, na wakakhiari upotovu kuliko uwongofu. Basi Mwenyezi Mungu amewalaani kwa ukafiri wao, na amedhoofisha yakini yao na imani yao.

89 Na Mtume wetu alipo wajia na Qur'ani, nayo ni Kitabu kilicho toka kwa Mwenyezi Mungu kinacho thibitisha Taurati walio teremshiwa wao, na wakajua kutokana na hiyo Taurati ukweli uliomo katika Kitabu hichi (Qur'ani) walikataa kwa inadi na uhasidi tu, kwa sababu yamekuja hayo kutokana na Mtume asiye kuwa wa taifa lao la Wana wa Israili, juu ya kuwa kabla yake walipo kuwa wakipambana na makafiri washirikina ikiwa mpambano wa vita au majadiliano, wakitaja kuwa Mwenyezi Mungu atakuja wanusuru wao kwa kumtuma Nabii wa mwisho aliye bashiriwa katika Kitabu chao, na ambaye sifa zake zimewafikiana kabisa moja kwa moja na sifa za Muhammad.(1) Jueni basi laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya watu wa namna hii wenye inda na ukanushi. (*Tazama Maelezo 2:89*)

90 Kiovu mmo walicho ziuza nafsi zao na roho zao! Na hayo ni kwa udhalimu wao, na kuona maya na kufanya uadui tu. Matamano yao na chuki zao za kikabila, na ugozi walio nao, ndio ulio wapelekea kukataa tulio yateremsha Sisi, kwa kuonea uchungu vipi Mwenyezi Mungu kumpa ujumbe wake Mtume asiye tokana na wao. Wanamkatalia Mwenyezi Mungu kuwa ni mwenye kukhiari atakavyo nani wa kumteremshia fadhila yake miongoni mwa waja wake. Kwa hivyo wamejipalilia wenyewe ghadhabu juu ya ghadhabu kwa kufuru zao na inadi zao na uhasidi wao. Na makafiri kama hawa watapata adhabu ya kuwadhalilisha na kutia uchungu.

91 . Hizi ndizo dhamiri walizo nazo ndani ya nafsi zao. Lakini mbele za watu wakijitetea kuwa wao hawaiamini Qur'ani wanapo takiwa waamini, kwa kuwa wao hawaiamini ila yale walio teremshiwa wao tu, na wanayakataa mengineyo. Na hakika wanasema uwongo kwa hayo madai yao kuwa wanaamini yaliyomo katika Taurati, kwani kwa kukitaa Kitabu hichi cha Qur'ani kinacho thibitisha Kitabu chao, ndio kuwa maana yake wanakataa Kitabu chao chenyewe, na kwa kuwa wao waliwauwa Manabii walio kuwa wanawaitia yale walio teremshiwa. Na wao kuwauwa hao ni dalili ya kukata kuwa hawauamini Ujumbe wao.

- 92.** Na alikufikieni Musa na hoja zilizo waziwazi, kisha mkamchukua ndama (kumuabudu) baada yake, na mkawa wenye kudhulumu.⁹²
- 93.** Na tulipo chukua ahadi yenu na tukauinua mlima juu yenu (tukakwambieni): Kamateni kwa nguvu haya tuliyo kupeni na sikieni. Wakasema: Tumesikia na tumekataa! Na wakanyweshwa nyoyoni mwao (imani ya) ndama kwa kufuru yao. Sema: Ni uovu mno iliyo kuamrisheni imani yenu ikiwa ni wenye kuamini.⁹³
- 94.** Sema: Ikiwa nyumba ya Akhera iliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni yenu tu bila ya watu wengine, basi tamanini mauti kama nyinyi mnasema kweli.⁹⁴
- 95.** Wala hawatayatamani kamwe kwa sababu ya yale yaliyo tangulizwa na mikono yao; na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwajua vyema wanao dhulumu.⁹⁵
- 96.** Na hakika utawaona ni wenye kuwashinda watu wote kwa pupa ya kuishi, na kuliko washirikina. Kila mmoja wao anatamani lau angeli pewa umri wa miaka elfu. Wala hayo ya kuzidishiwa umri hayamuondoshei adhabu; na Mwenyezi Mungu anayaona wanayo yatenda.⁹⁶
- 97.** Sema: Aliye kuwa ni adui wa Jibril, basi huyo ndiye aliye iteremsha Qur'ani moyoni mwako kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, inayo thibitisha yaliyo kuwa kabla yake, na ni uwongofu na bishara njema kwa Waumini.⁹⁷
- 98.** Aliye kuwa adui wa Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Mitume wake na Jibril

92 Bali hakika nyinyi Mayahudi mlikanusha kwa uwazi Vitabu vyenu, na mkarejea katika ushirikina katika zama za Musa mwenyewe. Kwani Musa alikujieni na hoja zilizo wazi, na miujiza inayo hakikisha ukweli wake, lakini kiasi ya kukupeni mgongo tu alipo kwenda kusema na Mola wake Mlezi nyinyi mkaingia kuabudu ndama, na mkarajea katika ukafiri wenu wa kuabudu masanamu, na nyinyi mkawa mlio dhulumu mlio potea.

93 Na alipo kuleteeni Taurati mkaziona amri ngumu ziliomo ndani yake, mkaona mizito mizigo yake na mkaitilia shaka, Mwenyezi Mungu alikuonyesheni Ishara ya ukweli wa Kitabu hicho na faida ya mafunzo yake kwenu. Akaunyanyua Mlima wa T'uur juu ya vichwa vyenu hata ukawa kama kiwingu, na mkadhani kuwa utakuangukieni. Hapo mkaonyesha kukubali na kut'ii. Tukachukua ahadi yenu kuwa hamtaghurika na pumbao katika kufuata yaliyomo katika Kitabu hichi. Mkasema: Tumeamini na tumesikia. Lakini vitendo vyenu vimefichua uasi wenu, na kwamba imani haijaingia katika nyoyo zenu. Wala hayumkini kuwa imani imeingia katika nyoyo za watu walio shughulishwa na mapenzi ya kumuabudu ndama. Imani yenu hiyo mnayo dai basi imekusozeni kwenye maovu

94 Na nyinyi mmedai kuwa Mwenyezi Mungu atakupeni nyinyi tu neema za Pepo baada ya kufa, wasipate watu wote wengineo. Ikiwa basi kweli mnaamini hayo myasemayo basi yafaa myapende mauti. Hebu yatamanini myapate upesi zisije kutaakhari hizo starehe mnazodai.

95 Lakini kwa hakika mambo yalivyo, wao hawayatamani mauti kabisa kwa dhulma walio ifanya, ambayo haifichikani kwa Mwenyezi Mungu. Yeye anawajua kuwa wao ni waongo kwa hayo wanao dai. Neema za Siku ya Kiyama zitakuwa ni za wachamngu, si za wafanyao maovu kama wao.

96 Bila ya shaka yoyote utawakuta wao ndio wamewashinda watu wote kwa pupa waliyo nayo kuwania maisha ya dunia ya kila namna, ya utukufu na unyonge. Na hiyo pupa yao inashinda ya makafiri washirikina (mapagani) wasio amini kufufuliwa wala Pepo. Kwa hivyo wanapenda lau kuwa wangelizidishiwa umri wakaishi hata miaka elfu. Na hata wangelishi vipi hawawezi kuepuka adhabu ya Mwenyezi Mungu inayo wangojea. Kwani Yeye ni Mjuzi wa hao madhaalimu, na atawaonjesha malipo ya vitendo vyao wanavyo vitenda

97 Na baadhi yao wanadai kuwa wanakupinga na wanakitataa Kitabu chako kwa kuwa ati wao ni maadui wa Jibril anaye kufikishia hichi Kitabu. Basi sema ewe Nabii uwaambie: Anaye kuwa Jibril ni adui wake, basi vile vile huyo ni adui wa Mwenyezi Mungu, kwa sababu Jibril haji na Kitabu hichi kwa nafsi yake, bali anakiteremsha kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Na Kitabu hichi kinathibitisha Vitabu vilivyo tangulia kutoka mbinguni. na kinathibitisha Kitabu chenu wenyewe. na hii Qur'ani (inayo teremshwa na Jibril kutoka kwa Mwenyezi Mungu) ni Uwongofu na Bishara njema kwa Waumini.

na Mikail, basi hakika Mwenyezi Mungu ni adui wa makafiri.⁹⁸

99. Hakika tumekuteremshia Ishara zilizo wazi na hapana wanao zikataa ila wapotovu.⁹⁹

100. Je! Ati ndio kila wanapo funga ahadi huwapo kikundi miongoni mwao kikaivunja? Bali wengi wao hawaamini.¹⁰⁰

101. Na alipo wajia Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye kuthibitisha yale waliyo nayo, kundi moja miongoni mwa wale walio pewa Kitabu lilitupa Kitabu cha Mwenyezi Mungu hicho nyuma ya migongo yao kama kwamba hawajui.¹⁰¹

102. Na wakafuata yale waliyo zua mashet'ani kuuzulia ufalme wa Su leiman. Na wala Suleiman hakukufuru, bali mashet'ani ndio walio kufuru, wakiwafundisha watu uchawi, na yaliyo teremshwa kwa Malaika wawili, Haaruta na Maaruta katika Baabil. Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru. Wakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe. Wala hawawezi kumdhuru mtu ila kwa kutaka Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza yatayo wadhuru wala hayawanufaishi. Na hakika wanajua kwamba aliye khiari haya hatakuwa na fungu lolote katika Akhera. Na hakika ni kiovu mno walicho jiuzia nafsi zao laiti wangelijua.¹⁰²

103. Na lau kuwa wangeamini na wakaogopa, bila ya shaka malipo yatokayo kwa

98 Basi yeyote anaye kuwa ni adui wa Jibril, au Mikail, au Malaika yeyote au Mtume yeyote, miongoni mwa Malaika na Mitume wa Mwenyezi Mungu, ambao hawafanyi kitu wala hawapeleki ujumbe ila kama vile Mwenyezi Mungu anavyo waamrisha, basi mtu huyo anakuwa ni adui wa Mwenyezi Mungu, na anakuwa kafiri anamkataa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni adui wa makafiri.

99 Na Jibril hateremshi kwenye moyo wako ila Ishara na hoja zilizo wazi, ambazo haiwezekani kwa mwenye kutafuta haki kikweli ila aziadini tu. Na hapana mwenye kuzikataa Ishara kama hizo ila wale wafanyao inda na inadi, ambao wametokana na mwenendo wa maumbile walio umbwa nao.

100 Na kama (hawa Wana wa Israili) walivyo kuwa vigeugeu katika itikadi na imani, hali kadhaalika walikuwa vigeugeu katika ahadi na mapatano wanayo choka nayo. Walikuwa kila wanapo fungamana na Waislamu au wengineo kwa maagano hutokea kikundi miongoni mwao wakavunjilia mbali maagano hayo. Kwani wengi wao hawaamini utukufu wa ahadi na utakatifu wa maagano.

101 Na alipo wajia Mtume aliye toka kwa Mwenyezi Mungu aliye wafikiana sawa sawa na sifa zilizo tajwa katika Vitabu vyao, naye ni Muhammad, rehema na amani iwe juu yake, kikundi kimojapo kutokana nao kilikataa hayo yaliyo tajwa katika Vitabu vyao kumkhusu Mtume huyu, kama kwamba halikutajwa jambo hilo humo wala wao hawajui lolote katika hayo.

102 Na wao hakika waliyasadiki waliyo yazua mashetani wao na wapotovu wao juu ya ufalme wa Suleiman, walipo dai kuwa Suleiman hakuwa Nabii wala si Mtume aliye teremshiwa ufunuo (Wahyi) kutoka kwa Mwenyezi Mungu, bali alikuwa ni mchawi tu anaye tegemea msaada wa uchawi wake. Na kwamba ni uchawi wake huu ndio ulio mjengea ufalme wake na ukamwezesha aweze kuwatawala majini, na ndege, na upepo. Kwa hivyo walimsingizia ukafiri Suleiman, na hali Suleiman hakukufuru, lakini hao mashetani waovu ndio walio kufuru. Wao ndio walio zua uzushi huu, wakaingia kuwafunza watu uchawi wao na walio pokea katika mabaki yaliyo teremka katika Baabil (Babilonia) kwa Malaika wawili, Haaruta na Maaruta. Na hawa Malaika wawili hawakuwa wakimfundisha mtu yeyote mpaka wamwambie: Sisi ni mtihani uwe ni majaribio kwenu, tunakufundisha mafunzo ambayo yanaweza kuleta fitna na ukafiri, basi jifunze lakini tahadhari usiitumie ilimu hii. Na lakini watu hawakunasihika kwa nasiha hii, na wakatamia hayo waliyo jifunza kwa hao Malaika wawili ya kumgombanisha mtu na mkewe. Naam, hawa mashetani waovu wamekufuru walipo zua katika uzushi wao na hadithi zao za uwongo wakafanya hayo ndio *wasila* na udhuru wa kuwafundishia Mayahudi uchawi. Na wao hao wachawi hawawezi kumdhuru yeyote, lakini Mwenyezi Mungu ndiye Yeye anayeweza kumletea mtu madhara pindi akipenda. Na hayo ya uchawi wao yanawadhuru hao wanao jifunza katika dini yao na dunia yao, na wala hawapati faida yoyote. Na wao wanajua kweli ya kujua ya kwamba anaye elekea upande huu hana sehemu yoyote katika neema za Akhera. Na kama wamebakia na ujuzi wowote yafaa wajue kuwa haya waliyo yakhiari kwa ajili ya nafsi zao ni hadi ya kuwa maovu.

Mwenyezi Mungu yange kuwa bora. Laiti wangeli kuwa wanajua!¹⁰³

104. Enyi mlio amini! Msiseme: “Raa’ina”, na semeni: “Ndhurna”. Na sikieni! Na makafiri watapata adhabu chungu.¹⁰⁴

105. Walio kufuru miongoni mwa watu wa Kitabu na washirikina hawapendi mteremshiwe kheri yoyote kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Na Mwenyezi Mungu humkusudia kumpa rehema yake ampendaye. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila kubwa.¹⁰⁵

106. Ishara yoyote tunayo ifuta au tunayo isahaulisha tunaitlea iliyo bora kuliko hiyo, au iliyo mfano wake. Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu?¹⁰⁶

107. Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ana ufalme wa mbingu na ardhi? Nanyi hamna mlinzi wala msaidizi isipo kuwa Mwenyezi Mungu.¹⁰⁷

108. Au mnataka kumwomba Mtume wenu kama alivyo ombwa Musa zamani? Na anaye badilisha Imani kwa ukafiri bila ya shaka huyo ameipotea njia iliyo sawa.¹⁰⁸

109. Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanatamani lau wange kurudisheni nyinyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu, kwa ajili ya uhasidi uliomo ndani ya nafsi zao, baada ya kwisha wapambanukia Haki. Basi sameheni na wachilieni mbali mpaka Mwenyezi Mungu atapo leta amri yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.¹⁰⁹

103 Na lau kuwa wameiamini Haki na wakauogopa ufalme na uwezo wa Mola wao Mlezi, basi Mwenyezi Mungu angeli walipa malipo mema, na hayo bila ya shaka yoyote yangeli kuwa ni bora zaidi kuliko wanayo yapata katika hadithi zao za uwongo na dhamiri zao mbovu wanazo zidhamiria, lau kuwa wanabagua linalo kuwa na manufaa wakaacha lenye madhara.

104 Enyi mlio amini! Tahadharini na hawa Mayahudi. Msimwambie Mtume pale anapo kusomeeni ufunuo: “Raa’ina” kwa kukusudia akuwekeni pahala pa uangalizi wake, yaani (Tuchunge, Turai), na akupeni muda katika kusoma kwake mpaka mzingatie na mhifadhi. Kwani watu makhabithi miongoni mwa Mayahudi husaidiana kutaka kukuigeni na kupindua ndimi zao kwa neno hilo mpaka likawa neno la matusi wanalo lijuu wao. Na wao humkabili Mtume kwa neno hilo kwa kumfanyia maskhara. Lakini nyinyi tumieni neno jingine wasilo weza Mayahudi kulipatia njia ya kufanya ukhabithi wao na maskhara yao. Tumieni neno: “Ndhurna” yaani “Tuangalie”. Na sikilizieni vyema anayo kusomeeni Mtume. Na Mwenyezi Mungu anawadundulizia adhabu kali kwa Siku ya Kiyama hawa wanao mfanyia maskhara Mtume. (*Tazama Maelezo 2:104*)

105 Na yafaa mjue kuwa hawa makafiri wa Kiyahudi na washirikina waabuduo masanamu hawakutakieni ila mdhurike tu, wala hawapendelei iteremke kheri yoyote kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Na Mwenyezi Mungu hathamini chochote wanacho kipenda wala wanacho kichukia. Kwani Mwenyezi Mungu humteua amtakaye kwa kumkhusisha kumpa rehema yake, na Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila kubwa.

106 Nao walikutaka wewe Muhammad, uwalettee miujiza, ishara, ile waliokuja nayo Musa na Manabii wa Wana wa Israili. Sisi yatutosha kuwa tumekutia nguvu kwa kukuletea Qur’ani. Na Sisi tunapo acha nguvu kumpa Nabii anaye kuja nyuma kwa muujiza wa Nabii aliyetangulia, au tukawasahaulisha watu athari za muujiza ule, basi Sisi humletea huyu Nabii aliyekuwa baadaye muujiza, kuwa ni Ishara, au Aya, iliyo bora zaidi au mfano wa ile ili kuwa ni dalili ya ukweli wake. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu. (Na hapana Ishara, Muujiza au Aya, iliyo kubwa na bora na yenye kudumu kuliko hii Qur’ani.)

107 Na Yeye, Mwenyezi Mungu, ndiye mwenye ufalme wa mbingu na ardhi katika mikono yake. Na nyinyi watu hamna mlinzi wa kukusaidieni, wala tegemeo la kukunusuruni isipokuwa Yeye.

108 Na kwa kule kumtaka kwenu Mtume wenu Muhammad miujiza fulani pengine ilikuwa mnawaiga Wana wa Israili wa zama za Musa, walipo mtaka uwalettee miujiza maalumu. Kutaka kwenu huku kunaficha nyuma yake inda na kumili kwenye ukafiri, kama kulivyo kuwa kule kutaka kwa Wana wa Israili kumtaka Mtume wao. Na mwenye kufuata nyayo za inda na ukafiri akaacha usafi wa kutaka Haki na Imani basi huyo ameipotea Njia iliyo sawa iliyo nyooka.

109 Na wengi miongoni mwa Mayahudi wametamani kukurejesheni, enyi Waislamu, kwenye ukafiri baada ya kuwa nyinyi mmekwisha amini. Na haya juu ya kuwa wao imekwisha wadhihirikia kutoka na

110. Na shikeni Sala na toeni Zaka; na kheri mtakazo jitangulizia nafsi zenu mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yafanya.¹¹⁰

111. Na walisema: Hataingia Peponi ila aliyekuwa Yahudi au Mkristo. Hayo ni matamano yao. Sema: Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli.¹¹¹

112. Sivyo hivyo! Yeyote anaye elekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu naye ni mtenda mema, basi ana malipo yake kwa Mola wake Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatuhuzunika.¹¹²

113. Na Mayahudi husema: Wakristo hawana lao jambo. Na Wakristo husema: Mayahudi hawana lao jambo. Na ilhali wote wanasoma Kitabu hicho hicho (Biblia). Na kadhaalika walisema wale wasio jua kitu mfano wa kauli yao hii. Basi Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyo kuwa wakikhitalafiana.¹¹³

114. Na ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye zuia misikiti ya Mwenyezi Mungu kutajwa ndani yake jina lake na akajitahidi kuiharibu? Watu hao haitawafalia kuingia humo ila nao wanaogopa. Duniani watapata hizaya na Akhera watapata adhabu kubwa.¹¹⁴

115. Na mashariki na magharibi ni za Mwenyezi Mungu. Basi kokote mnako elekea, huko Mwenyezi Mungu yupo. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa na Mjuzi.¹¹⁵

hicho hicho Kitabu chao kuwa nyinyi mpo juu ya Haki. Na hayakuwa hayo ila ni kuwa wanakuhusuduni na wanaogopa utawala usiwatoke mikononi mwao mkapewa nyinyi. Basi nyinyi wapuuzeni, na wasameheni, na waachilieni mbali mpaka Mwenyezi Mungu akuonyesheni lipi jengine la kuwafanyia, kwani Yeye ni Muweza wa kukupeni ushindi juu yao, na Yeye ni Muweza wa kila kitu.

110 Na hifadhini mambo ya Dini yenu: Shikeni Sala, toeni Zaka, na vitendo vyote vyote vyema mnavyo fanya kujitangulizia nafsi zenu, na sadaka mnazo toa, malipo yake mtayakuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua vyema myatendayo; ujuzi wake ni ujuzi wa mwenye kutazama akaona.

111 Na katika upotovu wa Mayahudi na Wakristo na matamano yao ya uwongo, ni yale madai ya kila mmoja wao kuwa hataingia Peponi ila mwenye kufuata dini yao. Hebu watakeni wa kutoleeni ushahidi wa hayo madai yao kama kweli wanasema kweli.

112 Na wala hawatapata ushahidi wa hilo. Kwani kweli ilivyo ni kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaandalia neema za Pepo, na atawalipa malipo Siku ya Kiyama, na atawalinda na khofu na huzuni, hao ambao wanao msafia niya Mwenyezi Mungu na wanafuata Haki, na vitendo wavitendavyo ni vyema.

113 Na ajabu iliyopo ni kuwa kama wanavyo fanyia uadui Uislamu, wanafanyiana uadui wenyewe, wao kwa wao. Mayahudi husema: Wakristo hawana lolote la haki. Na Wakristo nao wanasema mfano wa hayo, na huku wote wawili wanatoa ushahidi wao kutoka hivyo hivyo vitabu vyao vya Biblia wanavyoviamini wao wote. Na wale washirikina wa Kiarabu wasio jua chochote katika vitabu vilivyo teremshwa kwa Mayahudi na Wakristo husema maneno kama hayo. Na kwa hakika wote hao pamoja wamesema kweli, kwani hapana kikundi kimojapo katika wao kilicho kuwamo katika Haki. Na hayo yatabainika pale Mwenyezi Mungu atapo wahukumu Siku ya Kiyama katika zile khitalafu zao wanazo khitalafiana.

114 Katika yanayo dhihirisha uadui wa wao kwa wao na uadui wao wote kwa Waislamu, ni kule baadhi ya mataifa yao yalivyo kuwa yakiharibu mwahala mwa ibada ya mataifa mengineo, na vile wale washirikina walivyo kuwa wakiwazuia Waislamu wasiingie Msikiti Mtakatifu wa Makka. Na hapana kabisa mwenye kudhulumu zaidi kuliko azuiaye asitajwe Mwenyezi Mungu katika pahala pa ibada, na akafanya juhudi kutaka kupaharibu. Watu hao watapata hizaya duniani, na Akhera watapata adhabu kubwa. Haiwafalii wao kufanya ukhalifu kama huu muovu, bali iwapasavyo ni kulinda utakatifu wa pahala pa ibada, wala wasiingie humo ila kwa unyenyekevu na kukhofu, wala wasizuilie kutajwa jina la Mwenyezi Mungu ndani yake. (Na ufisadi kama huu, bali ni mkubwa zaidi, ni wa wale wanao ghusubu mali za wakfu ya misikiti.)

115 Ikiwa washirikina waliwazuia Waislamu kusali katika Msikiti Mtakatifu wa Makka, hawatoweza kuwazuia kusali na kumuabudu Mwenyezi Mungu. Kwani jiha zote na pande zote za dunia ni za Mwenyezi Mungu. Na hakika bila ya shaka Mwenyezi Mungu anampokelea Muislamu Sala zake, na

116. Na ati wanasema: Mwenyezi Mungu ana mwana. *Subhanahu!* Ametakasika na hayo. Bali vyote viliomo mbinguni na duniani ni vyake. Vyote vinamt'ii Yeye.¹¹⁶

117. Yeye ndiye Muumba wa mbingu na ardhi pasina ruwaza; na anapo taka jambo basi huliambia tu: Kuwa! Nalo huwa.¹¹⁷

118. Na walisema wale wasio jua kitu: Mbona Mwenyezi Mungu hasemi nasi au zikatufikia Ishara. Kama hivyo walisema wale walio kuwa kabla yao mfano wa kauli yao hii. Nyoyo zao zimefanana. Hakika Sisi tumeziweka wazi Ishara kwa watu wenye yakini.¹¹⁸

119. Hakika Sisi tumekutuma kwa Haki uwe mbashiri, na mwonyaji. Na wala hutaulizwa juu ya watu wa Motoni.¹¹⁹

120. Mayahudi hawawi radhi nawe, wala Wakristo, mpaka ufuate mila yao. Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu. Na kama ukifuata matamaniao yao baada ya ujuzi ulio kwisha kujia, hutapata mlinzi wala msaidizi kwa Mwenyezi Mungu.¹²⁰

121. Wale tulio wapa Kitabu, wakakisoma kama ipasavyo kusomwa, hao ndio kweli wanakiamini. Na wanao kikataa basi hao ndio wenye kukhasiri.¹²¹

122. Enyi Wana wa Israili! Kumbukeni neema yangu niliyo kuneemesheni, na hakika Mimi nikakufadhilisheni kuliko wengineo wote.¹²²

anamkabili kwa radhi yake pande zote anapo fanya ibada yake. Kwani Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa, hawadhikishi waja wake, na Yeye ni Mwenye kujua vyema niya ya mwenye kumuelekea.

116 Basi huyo ambaye mambo yake ni kama hivi, na vyote viliomo ulimwenguni vinat'ii amri yake, vinanyenyekea kwa atakalo, basi Yeye huyo yuko juu mno, na mtukufu mno hata habitajii kuwa na dhuriya au kujipa wana, kama wanavyo zua hawa Mayahudi na Wakristo na washirikina mapagani.

117 Vipi awe na haja ya uzazi au atafute mwana huyo aliye anzisha kuumba mbingu na ardhi bila ya kuwa na kiigizo chochote kabla yake, na akavifanya vyote viliomo humo vimt'ii Yeye kwa kila atakalo, na visiweze kumuasi? Yeye akitaka kitu basi husema tu: Kuwa! Kikawa.

118 Washirikina wa Kiarabu walikakamia katika inadi yao kumfanyia Muhammad, wakamtaka kama wale kaumu zilizo tangulia zilivyo wataka Manabii wao. Wakasema kuwa hawatomuamini ila Mwenyezi Mungu aseme nao, na awalettee ishara, au muujiza wa kuona utakao oneshwa ukweli wake. Haya ni kama walivyo sema Wana wa Israili kumwambia Musa: Hatukuamini mpaka tumwone Mwenyezi Mungu na aseme nasi. Na kama masahaba (wanafunzi) wa Isa walipo mtaka awateremshie chakula kutoka mbinguni. Na haya yote ni kuwa nyoyo za makafiri na wapinzani wenye inda katika kila umma zimefanana. Haki haidhihiriki ila kwa wale ambao kuona kwao kumesafika, na akili zao zimeelekea kufuata Yakini, na kuitaka Haki.

119 Na Sisi tumekutuma ufikishe Haki iliyo yakini ili uwape bishara njema Waumini, na uwaonye makafiri. Na waajibu wako ni kufikilisha tu ujumbe wetu, wala wewe hutosailiwa kwa kukosa Imani hao wasio kuamini, ambao wataingia Motoni.

120 Basi usjikere nafsi yako kwa kutaka kuwaridhi hao wapinzani wa Kiyahudi na Wakristo. Kwani hao hawatakuwa radhi nawe mpaka ufuate mila yao hao ambao wanadai ati ndio wenye uwongofu. Na kabisa hapana uwongofu ila uwongofu wa Mwenyezi Mungu ulioko katika Uislamu. Na mwenye kufuata matamaniao ya watu hawa baada ya kujua Haki tulio kuteremshia wewe, basi Siku ya Kiyama hatapata mlinzi wa kumsaidia mbele ya Mwenyezi Mungu, wala hatapata wa kumnusuru na adhabu.

121 Tena kipo kikundi katika Mayahudi na Wakristo walio wataalamu katika vitabu vyao vya asli, na wakavisoma vilivyo, na wakafahamu mageuzo yaliomo ndani yake, hao wanauamini ukweli wa mambo, na kwa hivyo wanaiamini hii Qur'ani. Na wenye kukikataa Kitabu kilicho teremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu hao ndio wenye kukhasiri.

122 Enyi Wana wa Israili! Aminini na mkumbuke neema kubwa niliyo kupeni kwa nilivyo kutoeni kwenye dhulma ya Firauni na nilivyo mzamisha baharini, na nilivyo kupeni Manna na Salwa, na nikakuleteeni Manabii kutokana miongoni mwenu, na nikakufunzeni Kitabu, na mengi mengineyo ya utukufu niliyo kupeni. Pia nikakunyanyueni kwa wakati fulani kuliko watu wote kwa vile nilivyo wateuwa Manabii

123. Na iogopeni siku ambayo hatamfaa mtu mwenziwe kwa lolote, wala hakitakubaliwa kwake kikomboleo, wala maombezi hayatamfaa, wala hawatanusuriwa.¹²³

124. Na Mola wake Mlezi alipo mjaribu Ibrahim kwa kumpa amri fulani, naye akazitimiza, akamwambia: Hakika Mimi nitakufanya uwe mwongozi wa watu. Akasema: Je, na katika vizazi vyangu pia? Akasema: Ahadi yangu haitawafikia wenye kudhulumu.¹²⁴

125. Na kumbukeni tulipo ifanya ile Nyumba (ya Alkaaba) iwe pahala pa kukusanyikia watu na pahala pa amani. Na alipo kuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia. Na tuliagana na Ibrahim na Ismail: Itakaseni Nyumba yangu kwa ajili ya wanao izunguka kwa kut'ufu na wanao jitenga huko kwa ibada, na wanao inama na kusujudu.¹²⁵

126. Na alipo sema Ibrahim: Ee Mola wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na uwaruzuku watu wake matunda, wale wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Akasema: Na mwenye kukufuru pia nitamstarehesha kidogo, kisha nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea.¹²⁶

127. Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipo inyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe ndiye Msikizi Mjuzi.¹²⁷

128. Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu kwako, na pia miongoni mwa vizazi vyetu wawe umma ulio silimu kwako. Na utuonyeshe njia za ibada yetu na utusamehe. Bila shaka Wewe ndiye Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.¹²⁸

kadhaa kutokana nanyi.

123 Na iogopeni adhabu ya Mwenyezi Mungu katika siku ambayo hapana mtu ataye weza kumtetea mwenziwe kwa lolote, wala fidia haitakubaliwa, wala maombezi hayatafaa kitu, wala makafiri hawatapata mtu wa kuwanusuru na Mwenyezi Mungu.

124 Na kumbukeni pale Mwenyezi Mungu alipo mjaribu babu yenu Ibrahim kwa kumtwisha amri fulani. Naye Ibrahim alizitimiza hizo amri vilivyo. Mwenyezi Mungu akamwambia: Mimi nataka kukufanya wewe uwe Imamu, yaani Mwongozi, wa watu, nao wawe wakikufuata wakishika nyayo zako. Ibrahim akamtaka Mola awajaalie katika vizazi vyake wawe pia Maimamu kama yeye. Mwenyezi Mungu akamjibu kuwa haya hawatayapata wanao dhulumu, na hivyo kaashiria kuwa mnamo dhuriya za Ibrahim watatokea walio wema na walio wabaya.

125 Na kadhaalika kumbukeni hadithi ya Ibrahim na mwanawe Ismail walipo ijenga ile Nyumba Takatifu ya Makka, Alkaaba. Katika kisa hichi pana funzo linalo fika mbali kwa mwenye moyo wa kuzingatia. Basi kumbukeni tulipo ifanya Nyumba hii ni pahala wanapo kwenda viumbe kutoka kila pahala duniani na kukusanyika. Na tukaifanya kuwa ni pahala pa usalama na amani kwa kila mwenye kutaka hifadhi. Na pia tulivyo amrisha kuwa pahala alipo kuwa akisimama Ibrahim kuijenga hiyo Nyumba pafanywe ni msala, yaani pahala pa kusalia. Na tukaagana na Ibrahim na Ismail waihifadhi Nyumba hiyo isipate kitu ambacho hakistahiki na utakatifu wake, na waitayarisha kwa matayarisho yanayo silihi kwa wanao kusanyika huko, wale wanao kwenda kut'ufu, na wanao kaa kwa ibada ya ii'tikafu, na wanao sali.

126 Na kumbukeni Ibrahim alipo mwomba Mola wake Mlezi ajaalie mji utakao kuwapo hapo kwenye nyumba ya Alkaaba uwe mji wa amani, na awaruzuku matunda ya ardhi na kheri zake watu wake watao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya mwisho. Mwenyezi Mungu alimjibu kuwa hatamnyima riziki hata kafiri muda wa uhai wake mfupi, kisha Siku ya Kiyama atakwenda ingia katika adhabu ya Jahannam, na mwisho wa watu hao ni muovu mno.

127 Na alipo kuwa Ibrahim na mwanawe Ismail wananyanyua misingi ya Alkaaba na huku wakimwomba Mwenyezi Mungu: Mola Mlezi wetu, Ewe Muumba wetu, na Muanzishi wetu! Tupokelee hii kazi yetu tuifanyayo kwa usafi wa niya kwa ajili yako, kwani Wewe ni Mwenye kusikia maombi yetu, ni Mwenye kujua ukweli wa niya yetu.

128 Mola Mlezi wetu! Tuwezeshe na utujaalie tuwe wenye kukusafia niya Wewe, na miongoni mwa vizazi vyetu wajaalie watoke watu wenye kukusafia Wewe. Na tufundishe njia za ibada yetu kukuabudu Wewe katika Nyumba hii takatifu na pembezoni mwake, na pokea toba yetu tunapo sahou au tunapo

129. Ewe Mola Mlezi wetu! Waletee Mtume anaye tokana na wao, awesomee Aya zako, na awafundishe Kitabu na hikima na awatakase. Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹²⁹

130. Na nani atajitenga na mila ya Ibrahim isipo kuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu? Na kwa yakini Sisi tulimteuwa yeye katika dunia; na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema.¹³⁰

131. Na Mola wake Mlezi alipo mwambia: Silimu, Nyenyekea! Alinena: Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote.¹³¹

132. Na Ibrahim akawausia wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu.¹³²

133. Je! Mlikuwapo yalipo mfikia Yaaqub mauti, akawaambia wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is-hak, Mungu Mmoja tu, na sisi tunasilimu kwake.¹³³

134. Hao ni watu walio kwisha pita. Watapata waliyo yachuma, nanyi mtapata mtakayo yachuma; wala hamtaulizwa nyinyi waliyo kuwa wakiyafanya wao.¹³⁴

135. Na wakasema: Kuweni Mayahudi au Wakristo ndio mtaongoka. Sema: Bali tunashika mila ya Ibrahim mwongofu, wala hakuwa katika washirikina.¹³⁵

kosea. Hakika Wewe ni mwingi wa kupokea toba za waja wako, na Msamehevu kwao kwa fadhila yako na rehema yako.

129 Mola Mlezi wetu! Waletee kutokana na vizazi vyetu Mtume miongoni mwao atakaye wasomea Aya zako na atawafundisha yale utakayo mfunulia yeye katika Kitabu na ilimu zenye manufaa na sharia zenye hikima, na awatakase kutokana na tabia mbovu. Hakika Wewe ndiye Mwenye kushinda, Mwenye nguvu, Mwenye hikima katika uyatendayo na unayo yaamrisha na unayo yakataza. (*Tazama Maelezo 2:129*)

130 Aliyo yafanya Ibrahim na aliyo yaomba kwa Mwenyezi Mungu ni mambo mazuri mno. Hali kadhaalika mila aliyo ifuata ni mila iliyo kwenda sawa kabisa. Na hapana anaye jitenga na mila ya Ibrahim ila mwenye kuudharau utu wake mwenyewe na akili yake. Hakika Mwenyezi Mungu alimteuwa yeye Ibrahim katika dunia, na pia Akhera ni miongoni mwa watu wema walio karibishwa.

131 Yeye Ibrahim alitikia amri ya Mola wake Mlezi pale alipo mtaka asilimu, yaani anyenyekee. Akasema: Namnyenyekea Mola Mlezi wa walimwengu wote, majini, watu na Malaika.

132 Na Ibrahim hakutosheka na hayo tu, bali aliwauusia wanawe wende mwendo wa uwongofu kama wake. Na mjukuu wake Yaakubu akamuiga, naye akawausia wanawe kadhaalika wafuate mwenendo huo huo. Aliwabainisha wanawe ya kwamba Mwenyezi Mungu amewateulia Dini ya Tawhidi, ya Mungu Mmoja. Na akachukua kwao ahadi kuwa hawatakufa ila nao ni Waislamu, wenye kuthibiti juu ya Dini hii.

133 Na nyinyi Mayahudi mlidai kuwa nyinyi mnakwenda mwendo wa Dini aliyo kufa nayo Yaakubu. Kwani nyinyi mlikuwapo pale mauti yalipo mjia Yaakubu hata mkajua kuwa alikufa katika mila gani? Basi zindukaneni mjue ya kuwa Yaakubu na wanawe walikuwa Waislamu wenye kumuamini Mungu Mmoja, wala wao hawakuwa Mayahudi kama nyinyi, wala hawakuwa Wakristo. (“Uyahudi” umeanza kuitwa hivyo baada ya Yuda, mwana wa Yaakubu. “Ukristo” ni baada ya Isa Masihi, Yesu Kristo. Ama “Uislamu”, yaani unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, ni Dini ya maumbile, ipo milele.) Na mjue ya kuwa Yaakubu alipo kabiliwa na mauti aliwakusanya wanawe na akawaambia: Mtaabudu nini baada yangu? Na wao wakajibu: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa baba zako Ibrahim na Ismail na Is-hak, Mungu Mmoja; na kwake Yeye tunanyenyekea.

134 Tena imekuwaje enyi Mayahudi kujadili mambo ya watu hawa? Hao ni watu walio kwisha pita na njia yao. Tena wao peke yao watawuna yale waliyo yatenda katika maisha yao. Nyinyi, basi, hamtaulizwa kitu juu ya vitendo vyao, na wala nyinyi hamtapata faida yoyote katika hayo. Nanyi hamtavuna ila yale matunda ya vitendo vyenu mnavyo vitenda nyinyi wenyewe.

135 Lakini wao hawaachi kuendelea katika ghasia na inda zao. Kila kikundi katika hao hudai kuwa ni dini yao wao tu ndiyo iliyo sawa. Mayahudi hukuambieni: Kuweni Mayahudi mpate kuhidika na kuongokewa kwenye njia sawa. Na Wakristo nao wanasema: Kuweni Wakristo ndio mpate kuongoka kwenye haki

136. Semeni nyinyi: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyo teremshiwa sisi, na yaliyo teremshwa kwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yaakub na wajukuu zake, na waliyo pewa Musa na Isa, na pia waliyo pewa Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi; hatutafautishi baina ya yeyote katika hao, na sisi tumesilimu kwake.¹³⁶

137. Basi wakiamini kama mnavyo amini nyinyi, itakuwa kweli wameongoka. Na wakikengeuka basi wao wamo katika upinzani tu. Na Mwenyezi Mungu atakutosheni kukukingeni na shari yao, na Yeye ndiye Msikizi, Mjuzi.¹³⁷

138. Huko ndiko kupaka rangi kwa Mwenyezi Mungu, na nani aliye mbora wa kupaka rangi kuliko Mwenyezi Mungu? Na sisi ni wenye kumuabudu Yeye tu.¹³⁸

139. Sema: Mnahojiana nasi juu ya Mwenyezi Mungu, naye ni Mola wetu Mlezi na Mola wenu Mlezi, na sisi tuna vitendo vyetu na nyinyi mna vitendo vyenu? Nasi tunamsafia Yeye tu.¹³⁹

140. Au mnasema kuwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yaakub na wajukuu zao walikuwa Mayahudi au Wakristo? Sema: Je, nyinyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu? Na ni nani mwenye kudhulumu zaidi kuliko yule aliye ficha ushahidi alio nao utokao kwa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na hayo myafanyayo.¹⁴⁰

iliyo nyooka. Nyinyi wajibuni kuwa sisi hatufuati hii wala hii kwa sababu dini zote hizo mbili zimekwisha potoka na zimeacha ile asli yake ya kweli, na zimeingia ndani yake ushirikina (upagani), na ziko mbali kabisa na mila ya Ibrahim. Bali sisi tunaufuata Uislamu ndio ulio ifanya mila ya Ibrahim kuwa safi iliyo safika.

136 Waambieni: Sisi tunamuamini Mwenyezi Mungu, na tunaamini Qur'ani iliyo teremshwa kwetu, na kadhaalika tunaamini waliyo teremshiwa Ibrahim, na Ismail, na Is-hak, na Yaakub na watoto na wajukuu zao, na tunaamini Taurati ile Mwenyezi Mungu aliyo mteremshia Musa ambayo iliyo kuwa haijakorogwa, na Injili aliyo teremshiwa Isa na Mwenyezi Mungu, ambayo haikukorogwa, na walio pewa Manabii wote kutokana na Mola wao Mlezi. Sisi hatutafautishi hata mmoja kati yao, tukawa tunawakanusha baadhi na kuwaamini wengineo. Na katika haya sisi tunakuwa ndio Waislamu wenye kunyenyekea amri ya Mwenyezi Mungu.

137 Wao wakiamini imani inayo wafikiana na imani yenu basi kweli wameongoka. Lakini wakikakamia katika inadi yao na kukataa kwao basi hao wamo katika ushindani usio koma, na hawana masikizano nanyi. Mwenyezi Mungu atakutosheni kukulindeni na shari yao, ewe Nabii. Na atakupumzisha na ghasia zao za inadi na upinzani wao. Kwani Yeye ni Mwenye kuyasikia wayasemayo, na Mwenye kuyajua hata yaliomo vifuani mwao.

138 Waambieni: Hakika Mwenyezi Mungu ametuongoa sisi kwa uwongofu wake mwenyewe, na ametuonyesha hoja zake. Na hapana mbora zaidi kwa uwongofu na hoja kuliko Mwenyezi Mungu. Na sisi hatumnyenyekei ila Mwenyezi Mungu. Na wala hatufuati ila anavyo tuongoa na kutuongoza Yeye. (Hilo ndilo pambo, au batizo, au kutia rangi kwa Mwenyezi Mungu--*S'ibghatu Llahi*).

139 Waambieni: Mnajadiliana nasi katika mambo ya Mwenyezi Mungu mkidai kuwa Yeye hakuteuwa Manabii ila kutokana nanyi tu? Na Mwenyezi Mungu ni Mola Mlezi wenu na Mola Mlezi wa kila kitu; hawapendelei kaumu fulani akawatupa wengine. Rehema yake humfikia amtakaye, na huwalipa watu wote kwa vitendo vyao, bila ya kuangalia nasaba yao na ukoo wao. Na Yeye ametuongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka katika vitendo vyetu. Na ameturuzuku tumsafie niya na vitendo Yeye.

140 Waambieni: Mnajadiliana nasi katika mas-ala ya Ibrahim, na Ismail, na Is-hak, na Yaakub na watoto na wajukuu zao, mkidai kuwa wao walikuwa Mayahudi au Wakristo kama nyinyi, na ilhali Sisi hatukuiteremsha Taurati na Injili wanazo zitegemea Mayahudi na Wakristo ila baada ya hawa. Na Sisi tulikwisha waelezeni khabari ya hayo. Jee, nyinyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu? Bali hakika Mwenyezi Mungu amekwisha waambieni nyinyi hayo katika vitabu vyenu. Basi msifiche kweli iliyo andikwa katika hivi vitabu vyenu. Na nani dhaalimu mkubwa zaidi kuliko yule anaye ificha kweli inayo toka katika kitabu chake ambayo naye anajua. Na Mwenyezi Mungu atakulipeni kwa upotovu mnao ushikilia, kwani Mwenyezi Mungu haghafiliki na mnayo yatenda.

141. Hao ni watu walio kwisha pita. Wao watapata waliyo yachuma, na nyinyi mtapata mliyo yachuma, wala hamtaulizwa nyinyi yale waliyo kuwa wakifanya wao.¹⁴¹

142. WAPUMBAVU miongoni mwa watu watasema: Nini kilicho wageuza kutoka kibla chao walicho kuwa wakikielekea? Sema: Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; Yeye humwongoa amtakaye kwenye njia iliyo nyooka.¹⁴²

143. Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu. Na hatukukifanya kibla ulicho kuwa nacho ila tupate kumjua yule anaye mfuata Mtume na yule anaye geuka akarejea nyuma. Na kwa yakini hilo lilikuwa jambo gumu isipo kuwa kwa wale alio waongoa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuipoteza Imani yenu. Kwani Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watu na Mwenye kuwarehemu.¹⁴³

144. Kwa yakini tukiona unavyo geuza geuza uso wako mbinguni. Basi tutakuelekeza kwenye Kibla ukipendacho. Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu; na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu upande huo; na hakika wale walio pewa Kitabu wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao Mlezi. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na yale wanayo yatenda.¹⁴⁴

141 Tena imekuwaje nyinyi Mayahudi na Wakristo kuyajadili mambo ya watu hawa? Kwani watu hawa wamekwisha pita na njia zao. Wao watapata malipo ya a'mali yao waliyo itenda katika uhai wao, wala nyinyi hamtaulizwa juu ya a'mali zao, wala hamtafaidika kwa lolote katika hayo. Nanyi hamtapata malipo ila kwa vitendo mnavyo vifanya nyinyi wenyewe.

142 Hakika wale wachache wa akili walio potezwa na pumbao lao wasiweza kufikiri sawa na kuzingatia miongoni mwa Mayahudi, na Wakristo, na washirikina na wanaafiki, watachukizwa kuwaona Waumini wameacha kukielekea kibla cha Beitul Muqaddas (Yerusalemu) walicho kuwa wakikielekea kwanza katika Sala. Na wao wakiona kuwa hicho kinastahiki zaidi kuliko kibla kingine, yaani cha Alkaaba. Basi waambie, Ewe Nabii! Jiha zote ni za Mwenyezi Mungu. Hapana upande ulio bora kuliko mwengine kwa dhati yake, lakini Mwenyezi Mungu ndiye mwenyewe anachagua upande autakao uwe ni kibla cha Sala. Na Yeye kwa mapenzi yake huongoa kila umma katika wanaadamu kufuata njia iliyo sawa anayo ikhiari Yeye na anayo ikhusisha Yeye. Na sasa umekuja Ujumbe wa Muhammad unafuta risala zote zilizo tangulia, na Kibla cha sasa cha Haki ni hichi cha Alkaaba iliyopo Makka.

143 Na kwa ajili ya kutaka huku ndio tukakuongoeni kwenye Njia Iliyo Nyooka kabisa, na tukakujaalieni muwe Umma wa katikati ulio bora kwa muujibu tulivyo iwafikisha Dini sahihi na vitendo vyema, ili muwe wenye kuthibitisha Haki kwa mnasaba wa sharia zilizo tangulia, na ili Mtume awe mlinzi juu yenu, akikupeni nguvu kwa uwongozi wake kwa muda wa uhai wake, na kwa kufuata njia yake na mwendo wake baada ya kufa kwake. Ama kibla cha Beitul Muqaddas tulicho amrisha kifuatwe kwa muda fulani tulikifanya kuwa ni mtihani kwa Waislamu ili watambulikane wanao t'ii wakielekee kwa ut'iifu, na wenye kuchukuliwa na mori wao wa Kiarabu kwa kufuata nyao za Ibrahim tu waivunje amri ya Mwenyezi Mungu na kwa hivyo wapotelee njia ya upotovu. Na ilikuwa ile amri ya kuelekea Beitul Muqaddas ni katika mambo magumu ila kwa wale ambao wamejaaliwa kupata hidaya ya Mwenyezi Mungu. Ikawa kufuata amri hii miongoni mwa nguzo za Imani. Mwenye kuelekea kibla cha Beitul Muqaddas katika zama ilipo amrisha hayo hakupoteza Imani yake na ibada yake kwa upole na rehema ya Mwenyezi Mungu.

144 Na Sisi tulikuona vipi unazichungua mbingu asaa uteremke Wahyi (ufunuo) wa kugeuza Kibla cha Beitul Muqaddas ufuata cha Alkaaba ambacho unakipenda, kwa kuwa ndicho Kibla cha Ibrahim, baba wa Manabii, na baba wa Mayahudi na Waarabu. Na hapo pana Maqaamu Ibrahim, alipokuwa akisimama Ibrahim. Kwa hivyo hichi ni Kibla kilicho kusanya wote, ijapokuwa kinaacha kibla cha Mayahudi. Basi hivi sasa Sisi tunakupa lile ombi lako. Kwa hivyo katika Sala zako elekea Masjidil Haraam (Msikiti Mtakatifu). Na nyinyi Waumini, kadhaalika, elekeeni huko popote pale mlipo. Watu wa Kitabu wanao udhika kwa kukiacha kwenu Kibla cha Beitul Muqaddas wanajua katika vitabu vyao kuwa nyinyi ni watu wa Alkaaba. Na wanajua kuwa amri ya Mwenyezi Mungu inawakhusisha watu wa kila sharia na kibla chao. Na hii ni haki inayo tokana na Mola wao Mlezi. Lakini wao wanataka kukufitinisheni na kukutilieni shaka katika Dini yenu. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika nao, na Yeye atawalipa

145. Na hao walio pewa Kitabu, hata ukiwaletea hoja za kila namna, hawatafuata Kibla chako; wala wewe hutafuata kibla chao, wala baadhi yao hawatafuata kibla cha wengineo; na kama ukiyafuata matamaniao yao baada ya kukufikia ujuzi, hakika hapo utakuwa miongoni mwa wenye kudhullumu.¹⁴⁵

146. Wale tulio wapa Kitabu wanayajua haya kama wanavyo wajua watoto wao; na kuna kikundi katika wao huificha haki na hali wanajua.¹⁴⁶

147. Haki inatoka kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanao fanya shaka.¹⁴⁷

148. Na kila mmoja anao upande anao elekea. Basi shindanieni mema. Popote mlipo Mwenyezi Mungu atakuleteni nyote pamoja. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.¹⁴⁸

149. Na popote wendako elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu. Na hiyo ndiyo Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na mnayo yatenda.¹⁴⁹

150. Na popote wendako elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu. Na popote mlipo elekezeni nyuso zenu upande huo ili watu wasiwe na hoja juu yenu, isipokuwa wale walio dhulumu miongoni mwao. Basi msiwagope wao, lakini niogopeni Mimi-

kwa wayatendayo.

145 Na hakukua tutoridhika kwao Watu wa Kitabu nanyi ni kwa kudanganyikiwa ambako kwaweza kuondoka kwa hoja, bali kuudhika huko ni kwa inadi na kiburi. Kwa hivyo Ewe Mtume! Hata ukiwaletea kila hoja ya kukata kuwa Kibla chako ndicho cha kweli, hawakubali kukifuata Kibla chako. Ikiwa Mayahudi wangi wanatumai kuwa bado utarejea kwenye kibla chao, na wanatoa hiyo ni shuruti ya kusilimu kwao, basi wataunjika moyo, wala wewe hutofuata kibla chao. Na hao watu wa Kitabu kila kikundi chao kina kibla chake mbali. Wakristo hawafuata kibla cha Mayahudi, wala Mayahudi hawafuata kibla cha Wakristo, na kila mmoja kati yao anawaona wengine hawamo katika haki. Basi wewe thibiti hapo hapo kwenye Kibla chako, wala usiyaendekeze matamaniao yao. Kwani mwenye kuyafuata matamaniao yao baada ya kwisha pata ujuzi kuwa wao ni wapotovu, na kujua kuwa yeye yuko katika haki, basi huyo ni katika walio dhulumu na wenye kubobea katika dhulma. (*Tazama Maelezo 2:145*)

146 Na hakika Watu wa Kitabu wanajua kuwa huku kugeuza Kibla ni jambo la haki, na wanakutambua kuwa wewe ndiye Nabii aliye sifiwa katika vitabu vyao, na miongoni mwa sifa hizo kuwa atasali kuelekea Alkaaba. Na kujua kwao Unabii wako na kukijua Kibla chako ni sawa sawa wanavyo wajua watoto wao kwa uwazi kabisa. Lakini baadhi yao wanaificha kweli hii juu ya kuwa wanajua, kwa kufuata pumbao na chuki zao za upotovu kuwania mila zao kwa ajili ya kulinda madaraka yao, na wanatafuta hila za kukupotoeni nyie.

147 Na hakika Haki ni anayo kutolea Mwenyezi Mungu Mtukufu sio wanayo kupotoshelea watu wa Kitabu. Basi kuweni na yakini nayo, msiwe watu wenye kutia shaka shaka na kubabaika. Na katika hiyo Haki ni hii amri ya Kibla, basi endeleeni nayo wala msiwabali wapinzani.

148 Hakika Kibla hicho tulicho kuelekeza ndicho Kibla chako na Kibla cha Umma wako. Na hali kadhaalika kila umma una kibla chake unako elekea katika sala yao kwa mujibu wa sharia zilizo kwisha pita. Wala katika haya hapana kupikuana kwa ubora, na ama kupikuana kwa ubora ni kwa kutenda vitendo vya ut'iifu na a'mali za kheri. Basi kimbilieni kwenye kheri na mshindane kwa hayo. Mwenyezi Mungu atakuhisabuni kwa hayo, kwani Yeye atakukusanyeni nyote Siku ya Kiyama kutoka kokote mtapo kuwako. Wala hatamchopoka hata mmoja. Kila kitu kimo mkononi mwake, na katika hivyo ni amana, kuhuisha, kufufua na kukusanya.

149 Basi katika Sala zako popote pale ulipo uelekee Msikiti Mtakatifu, ukiwa upo mjini au umo safarini, popote wendapo. Na hakika haya bila ya shaka ndiyo ya Haki yanayo wafikiana na hikima ya Mola wako Mlezi aliye pamoja nawe. Basi wewe na umma wako yatamanini haya. Kwani Mwenyezi Mungu atakulipeni malipo mema kabisa. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye ujuzi wala hapana katika vitendo vyenu vilivyo fichikana naye.

na ili nikutimizieni neema yangu, na ili mpate kuongoka.¹⁵⁰

151. Kama tulivyo mtuma Mtume kwenu anaye tokana na nyinyi, anakusomeeni Aya zetu na kukutakaseni na kukufundisheni Kitabu na hikima na kukufundisheni mliyo kuwa hamyajui.¹⁵¹

152. Basi nikumbukeni nitakukumbukeni, na nishukuruni wala msinikufuru.¹⁵²

153. Enyi mlio amini! Takeni msaada kwa subira na Sala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri.¹⁵³

154. Wala msiseme kuwa wale walio uwawa katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni maiti; bali hao ni wahai, lakini nyinyi hamtambui.¹⁵⁴

155. Hapana shaka tutakujaribuni kwa chembe ya khofu, na njaa, na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wabashirie wanao subiri,¹⁵⁵

156. Wale ambao ukiwasibu msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.¹⁵⁶

150 Jilazimishe kuifuata amri ya Mwenyezi Mungu katika mambo ya kuelekea Kibla, na kuwa na pupa nayo wewe na umma wako. Na uelekeze uso wako uelekee upande wa Msikiti Mtakatifu popote wendapo katika safari zako. Na elekeeni huko popote mtapo kuwapo pande zote za dunia, mkiwa mko safarini au mpo mjini, ili ukatike ule ushindani wa hoja za hao walio khalifu na wanao jadiliana nanyi ikiwa hamkufuata amri hii ya kugeuza Kibla. Mayahudi watasema: Vipi Muhammad anapo sali anaelekea Beitul Muqaddas, na Nabii alielezwa katika vitabu vyetu ni kuwa moja katika sifa zake anaelekea Alkaaba? Na washirikina wa Kiarabu watasema: Vipi anadai kuwa mila yake ni mila ya Ibrahim, naye hafuati Kibla chake? Juu ya vyote hakika hao walio dhulumu walio potoka wakaiacha Haki kutoka pande zote mbili hawatoacha majadiliano yao na upotovu wao, bali watasema: Hakugeuka kuelekea Alkaaba ila kuwa anafuata ile ile dini ya kishirikina ya kaumu yake, na kuupenda ule mji wake. Basi nyinyi msiwabali hao, kwani uchochezi wao hauto kudhuruni. Nanyi niogopeni Mimi, msiikhalifu amri yangu. Kwa amri hii tumetaka kuitimiza neema juu yenu, na Kibla hichi tulicho kuelekezeni ndicho kipelekee kuthibiti kwenu katika uwongofu na kupata tawfiki.

151 Na hivi kukuelekezeni kwenye Msikiti Mtakatifu na kwa kuwa tumekutumieni Mtume aliye tokana nanyi, akikusomeeni Aya ni katika kukutimizieni neema yetu, kama tulivyo kutimizieni ile neema - nayo ni Qur'ani - na akusafishieni nafsi zenu zitoke uchafu wa ushirikina na tabia na ada mbovu mbovu, na anakusemezeni kwa njia ya kukufunzeni maarifa ya Qur'ani na ilimu zenye nafuu, na kukufunzeni mambo ambayo mlikuwa hamyajui. Kwani mlikuwa katika ujinga na upotovu ulio mpofu wa kijahilia.

152 Basi enyi Waumini! Nikumbukeni kwa kunit'ii, na Mimi nitakukumbukeni kwa kukupeni thawabu. Na nishukuruni kwa neema nilizo kuvikeni, wala msizipinge neema hizi kwa kuyaasi yale niliyo kuamrisheni.

153 Na tafuteni kujisaidia, enyi Waumini, katika kila linalo kupateni, kwa kusubiri na kushika Sala. Sala ndio msingi wa ibada zote. Hakika Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake wenye nguvu yu pamoja na wanao subiri. Yeye ndiye mlinzi wao, na Yeye ndiye anaye wanusuru daima.

154 Na subira haipolekei ila kwenye kheri na kufanikiwa kote kuwili, duniani na Akhera. Basi msikae nyuma mkaacha kwenda kupigana *Jihadi* kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Wala msiogope kufa katika Jihadi, kwani mwenye kufa katika Jihadi huyo si maiti, hakufa, bali yuhai maisha ya juu kabisa, ijapo kuwa hawa tunao waona wahai hawatambui hayo.

155 Subira ni ngao na silaha ya Muumini ambayo kwayo hushindia kila shida na mashaka. Na nyinyi zitakuja kupateni shida nyingi. Tutakujaribuni na kukufanyieni mitihani kwa vitisho vya maadui, kwa njaa, na uchache wa vifaa, na kupungukiwa mali, na watu kufa, na kupotea mazao. Na hapana la kukulindeni katika mitihani huu mkali ila Subira. Basi Ewe Nabii! Wape bishara nzuri wanao subiri kwa moyo na ulimi.

156 Wale ambao kwamba yanapo wateremkia machungu ya kuwaumiza wanaamini ya kuwa hakika kheri yote na shari inatokana na mwenyewe Mwenyezi Mungu, na ya kwamba amri yote ni ya Mwenyezi Mungu. Hao husema: Sisi ni milki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na sisi ni wenye kurejea kwake Yeye. Sisi hatuna letu jambo lolote. Na Yeye ni mwenye kustahiki kushukuriwa kwa anacho toa, na juu yetu kusubiri wakati wa kujaribiwa, na kwake Yeye ndiyo zipo thawabu na malipo.

157. Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao Mlezi na rehema. Nao ndio wenye kuongoka.¹⁵⁷

158. Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Basi anaye hiji kwenye Nyumba hiyo au akafanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka. Na anaye jitendea mwenyewe kheri basi bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye shukrani na Mjuzi.¹⁵⁸

159. Hakika wale wanao ficha tuliyo yateremsha -- nazo ni hoja zilizo wazi na uwongofu baada ya Sisi kuzibainisha kwa watu Kitabuni -- hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani kila wenye kulaani.¹⁵⁹

160. Ila wale walio tubu na wakatengeneza na wakabainisha, basi hao nitapokea toba yao, na Mimi ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu.¹⁶⁰

161. Hakika walio kufuru na wakafa hali ni makafiri, hao iko juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote.¹⁶¹

162. Watadumu humo. Hawata-punguziwa adhabu wala hawatapewa muda wa kupumzika.¹⁶²

163. Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hapana mungu ila Yeye. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.¹⁶³

164. Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na kukhitalifiana usiku na mchana, na marikebu ambazo hupita baharini kwa viwafaavyo watu, na maji anayo yateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa

157 Basi hao wenye kusubiri, wenye kumuamini Mwenyezi Mungu, wanapewa bishara njema kuwa watapata maghfira na ihsani ya Mwenyezi Mungu, na wao ndio wenye kuongoka njia ya kheri na uwongozi mwema.

158 Na kama alivyo kuwa Mwenyezi Mungu ametukuza hadhi ya Alkaaba akaifanya iwe ndiyo Kibla cha Sala, hali kadhaalika ametukuza shani ya vilima viwili vilipo Makka, navyo ni Safaa na Marwa, akavifanya miongoni mwa mahala pa kufanyia ibada ya Hijja. Basi imewajibikia baada ya kuizunguka Alkaaba kwa kut'ufu, kwenda huku na huku baina ya vilima viwili hivyo mara saba. Kwenda huko kunaitwa Sa'yu. Na baadhi yenu labda walikuwa wakiona vibaya kufanya hivyo kwa kuwa kilikuwa kitendo cha siku za jahiliya kabla ya kuja Uislamu. Lakini kweli iliopo ni kuwa hiyo ni ada ya Kiislamu ya tangu zamani. Basi hapana ubaya wowote kufanya Sa'yu baina ya vilima viwili hivi kwa mwenye kunuwiya Hijja na Umra. Na Muumini na afanye jambo la kheri kama awezavyo, kwani hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa ayatendayo, na Yeye atamlipa kwa a'mali yake.

159 Hao wanao kukatalieni Dini yenu wako makundi mawili: kundi moja ni katika Watu wa Kitabu wanao ijua Kweli, lakini wanaificha kwa kujua na kwa inda. Na kundi jengine ni la washirikina ambao nyoyo zao ni pofu, kwa hivyo hawaioni Kweli, na badala ya Mwenyezi Mungu Mmoja wakawa wanaabudu miungu myengineo. Basi Watu wa Kitabu walio jua ushahidi wa ukweli wako wanajua haki ya Dini yako, lakini kisha wanazificha hizo dalili ili watu wasijue. Mwenyezi Mungu atawapatiliza ghadhabu yake, na atawaepusha rehema yake, na kila wanao omba katika Malaika, na Wanaadamu na Majini watawaapiza wasipate rehema ya Mwenyezi Mungu.

160 Wala hapana atakaye vuka na laana hiyo katika wao ila aliye tubu na akatenda mema kwa kuacha kuficha Haki, akayadhihirisha aliyo kuwa akiyaficha katika sifa za Mtume na Uislamu. Mwenyezi Mungu atakubali toba yake na atamfutia dhambi zake, kwani Yeye ndiye anaye kubali toba ya waja wake kwa huruma na rehema yake.

161 Ama wale walio kakamia na ukafiri, na wakafa bila ya toba wala majuto, jaza yao ni laana ya Mwenyezi Mungu, na Malaika na watu wote.

162 Na wataendelea katika laana hii na katika Moto, wala hawatapunguziwa adhabu, wala hawatapewa muhula wala haitokhirishwa. Hata wakiomba muhula na kuakhirishwa hawataitikiwa.

163 Hakika Mungu wenu anaye stahiki kuabudiwa pekee ni Mmoja. Hakuna mungu mwengine, wala hapana utawala ila wake. Tena Yeye amesifika kuwa ni Mwenye rehema, basi Yeye ni Rahim, Mwenye Kuwarehemu waja wake katika kuwaumba na kuwafanya walivyo.

kwake, na akaeneza humo kila aina ya wanyama; na katika mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayo amrisha kupita baina ya mbingu na ardhi, bila shaka zimo Ishara kwa watu wanao zingatia.¹⁶⁴

165. Na katika watu wapo wanao chukua waungu wasio kuwa Mwenyezi Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walio amini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana. Na laiti walio dhulumu wakajua watakapo iona adhabu kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu na kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu!¹⁶⁵

166. Walio fuatwa watakapo wakataa wale walio wafuata, na hali ya kuwa wamekwisha iona adhabu; na yatakatika mafungamano yao.¹⁶⁶

167. Na watasema wale walio fuata: Laiti tungeweza kurudi tukawakataa wao kama wanavyo tukataa sisi! Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyo waonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni.¹⁶⁷

168. Enyi watu! Kuleni vilivyomo katika ardhi, halali na vizuri, wala msifuate nyayo za Shet'ani. Hakika yeye ni adui yenu aliye dhaahiri.¹⁶⁸

169. Yeye anakuamrisheni maovu na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu mambo msiyo yajua.¹⁶⁹

170. Na wanapo ambiwa: Fuateni aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu; wao husema: Bali tutafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa

164 Na zipo dalili nyingi na Ishara kwa kila mwenye akili juu ya kuwapo kwake na Ungu wake. Miongoni mwa hizo ni hizi mbingu mziyozoz zinazo pitiwa na sayari kwa nidhamu bila ya kuzahamiana wala kugongana, zikiuletea ulimwengu huu joto na nuru. Na pia hii dunia yenye bara na bahari, na kupishana usiku na mchana, pamoja na manufaa yake. Katika Ishara na dalili hizo ni kuzingatia marikebu zipitazo baharini zikibeba watu na vifao vyao, na hapana aziendeshao hizo ila Mwenyezi Mungu. Ni Yeye ndiye anaye zituma pepo zinazo leta mvua. Na mvua ikateremka ikahuisha wanyama na ikanywesha ardhi na mimea. Na hizo pepo kwa mivumo yake ya kila namna, na mawingu yaliyo tundikwa baina ya mbingu na ardhi: Jee, yote haya yamesimama kwa uangalifu namna hii na kwa hukumu kama hizi wenyewe tu? Au vimeundwa na Mwenye Kujua Mwenye Uwezo?

165 Na juu ya dalili zilizo wazi baadhi ya watu walio potelewa na akili wamewafanya miungu mingine isiyo kuwa Mwenyezi Mungu, wakiwat'ii na kuwaabudu kama Mwenyezi Mungu na wakawafanya mfano wa Mwenyezi Mungu. Muumini humuelekea Mwenyezi Mungu tu, na kumt'ii kwake hakuna ukomo. Ama hao ut'ifu wao kwa miungu yao hulegalega wakati wa shida. Hapo basi humkimbilia Allah *Subhanahu*. Na walio jidhulumu nafsi zao lau wangezingatia adhabu itakayo wapata Siku ya Malipo, utakapo dhihiri Ufalme wa Mwenyezi Mungu, na ut'ifu ukawa wake tu wangelichilia mbali ukhalifu wao na wangelisita kutenda dhambi zao.

166 Siku hiyo wafuasi watatamani wakubwa wao wawaokoe na upotofu, nao watawakataa na kujitenga nao wakisema: Hatukukwiteni mtut'ii katika kumuasi Mola wenu Mlezi. Hilo ni pumbao lenu tu na uovu wa vitendo vyenu. Makhusiano baina yao na mapenzi waliyo kuwa nayo duniani yatakatika siku hiyo, na watakuwa maadui wao kwa wao.

167 Na hapa wafuasi itawabainikia kuwa walipotea walipo wafuata viongozi wao katika upotovu, na watatamani warejee duniani wawakataa viongozi wao kama wao walivyo wakataa siku ya leo. Vitendo vyao viovu vitadhihiri wajute, lakini wapi! Vimekwisha watumbukiza Motoni, na wala hawatatoka humo.

168 . Enyi watu! Kuleni vyakula alivyo kuumbieni Mwenyezi Mungu katika ardhi vilivyo halali, visivyo harimishwa, vilivyo vizuri, vinavyo pendwa na nafsi. Wala msifuate Shetani anaye kupendezeni kula chakula cha haramu, au kuharimisha kilicho halali. Nyinyi mmeujua uadui wa Shetani kwenu, na umebainika ubaya wa anayo kuamrisheni.

169 Shetani anakupambieni kiovu kwa dhati na chenye madhara kwa afya yenu, na kibaya ili mkitende. Kwa sababu yake mnafuata dhana na mawazo yasio na msingi. Mkamsingizia Mwenyezi Mungu kuhlalisha na kuharimisha bila ya dalili ya ilimu na yakini.

hawaelewi kitu, wala hawakuongoka?¹⁷⁰

171. Na mfano wa walio kufuru ni kama mfano wa anaye mpigia kelele asiye sikia ila wito na sauti tu -- ni viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawaelewi.¹⁷¹

172. Enyi mlio amini! Kuleni vizuri tulivyo kuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa kweli mnamuabudu Yeye tu.¹⁷²

173. Yeye amekuharimishieni mzoga tu na damu na nyama ya nguruwe na kilicho tajiwa, katika kuchinjwa kwake, jina la asiye kuwa Mwenyezi Mungu. Lakini aliye fikiwa na dharura bila ya kutamani wala kupita kiasi, yeye hana dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.¹⁷³

174. Hakika wale wafichao aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu katika Kitabu, wakanunua kwacho thamani ndogo, hao hawali matumboni mwao isipo kuwa moto, wala Mwenyezi Mungu hatawasemeza Siku ya Kiyama, wala hatawatakasa. Nao watapata adhabu chungu.¹⁷⁴

175. Hao ndio walio nunua upotofu badala ya uwongofu, na adhabu badala ya maghira. Ama wavumilivu wa Moto watu hawa!¹⁷⁵

176. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ameteremsha Kitabu kwa haki. Na wale

170 Wapotovu walio acha njia ya uwongofu wamezoea kuyashika waliyo yarithi kwa baba zao katika itikadi na vitendo. Wanapo itwa wafuate uwongofu wa Mwenyezi Mungu husema: Hatuachi tuliyo yakuta kwa baba zetu. Katika ujinga mkubwa kabisa ni kukhiari kufuata wazee kuliko kumt'ii Mwenyezi Mungu na kufuata uwongofu wake. Kefu basi inapo kuwa baba zao hawanacho wakijuacho katika Dini, na hawana mwangaza wa kuwanawirisha uwongofu na Imani?

171 Na mfano wa kuwaita hao makafiri wanao pinga haki na uwongofu na wasiitikie wala wasifahamu wanaitiwa nini ni mfano wa mchungu kondoo anapo wasemeza hayawani. Hawafahamu kitu wala hawasikii ila sauti, wala hawaelewi kinginecho. Basi hao kadhaalika kwa mintarafu ya Haki ni viziwi wa kusikia, vipofu wa kuona, mabubu wa kusema. Hawatamki jema, wala hawatoi la akili.

172 Na Sisi tumewaruhusu watu kula kila kilicho halali tulicho waumbia katika ardhi. Na tumewakataza wasifuate nyayo za Shetani. Wakifanya hivyo watakuwa wameongokewa, lakini wakikataa basi Sisi tunawakhusisha Waumini tu kwa uwongofu wetu, na tunawabainisha wao kilicho halali na haramu. Basi enyi Waumini! Mmeruhusiwa kula kila chakula kitamu kilicho chema, sio kichafu. Basi mshukuruni Mwenyezi Mungu aliye kuwekeeni wazi neema ya kumakinika kwa vitu vizuri na kukuhalalishieni, na kwa neema ya ut'iifu na kufuata amri yake ili ibada zenu zitimie. (*Tazama Maelezo 2:172*)

173 Sio yaliyo harimishwa wanayo zua Washirikina na Mayahudi. Lakini mlicho harimishiwa nyinyi Waumini ni nyamafu, mzoga, yaani mnyama asiye chinjwa, na mfano wake katika kuharimishwa ni nyama ya nguruwe, na nyama ambaye wakati wa kuchinjwa ametajiwa jina lisilo kuwa la Mwenyezi Mungu, kama vile miungu ya uwongo au mfano wake. Juu ya hivyo mtu akilazimika kwa dharura kula kidogo katika vilivyo katazwa kwa ajili ya njaa, na hakupata kinginecho, au kwa kulazimishwa, basi hana makosa juu yake. Lakini ajitenge na mwendo wa kijaahili, kutaka kula vilivyo katazwa kwa kutamani tu, na wala asipite kiasi kula kuliko cha kuondoa njaa tu. (*Tazama Maelezo 2:173*)

174 Miongoni mwa watu wanao jua aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu kipo kikundi kinacho ficha baadhi ya maandishi ya ufunuo kwa ajili ya sababu fulani za kilimwengu. Mayahudi, mathalan, wakificha mengi yaliyo kuja katika Taurati ya kueleza sifa za Mtume kwa kukhofu wasije wakashilimu watu wa mila yao na kwa hivyo utukufu wao ukaondoka na wakapoteza mapato yao na vyakula vyao vitamu. Na hakika chakula chao wakilacho kwa njia hii ni kama kula moto, kwani hayo yatawapelekea kuingia Motoni. Mwenyezi Mungu atawatupilia mbali Siku ya Kiyama, wala hatawasafisha uchafu wao, na mbele yao kuna adhabu ya kuumiza kweli.

175 . Hao ndio wenye madhambi walio khiari upotovu wakaacha uwongofu, na kwa hivyo wakastahiki adhabu ya Akhera badala ya kupata msamaha. Watakuwa kama mwenye kununua baat'ili kwa haki, na chenye upotovu kwa chenye uwongofu. Hakika hali yao ni ya kustajabisha, kwa kuwa wanavumilia kufanya mambo ambayo hayana budi kuwapelekea kwenye adhabu, na tena wakawa wenyewe wakayaonea uzuri hayo yanayo wapeleka huko!

walio khitilafiana katika Kitabu wamo katika upinzani ulio mbali na haki.¹⁷⁶

177. Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao.¹⁷⁷

178. Enyi mlio amini! Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika walio uwawa - muungwana kwa muungwana, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke. Na anaye samehewa na ndugu yake chochote basi ashikwe kulipa kwa wema, na yeye alipe kwa ihsani. Huko ni kupunguziwa kuliko tokana na Mola wenu Mlezi, na ni rehema. Na atakaye vuka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu chungu.¹⁷⁸

179. Mtakuwa nao uhai mzuri katika kulipiza kisasi enyi wenye akili, ili msalimike.¹⁷⁹

180. Mmeandikiwa -- mmoja wenu anapo fikwa na mauti, kama akiacha mali -- afanye

176 Nao yamewapasa malipo waliyo kadiriwa kwa kukikataa Kitabu cha Mwenyezi Mungu alichokiteremsha kwa haki na kweli. Na wamekhitilafiana kwacho khitilafu kubwa iliyo wapelekea kupenda kujadiliana na kujitenga na Haki, na kufuata pumbao, wakakigeuza na kukifisidi na kukifasiri kinyume na maana yake ya hakika.

177 Watu wamekithirisha maneno juu ya Kibla kama kwamba wema wote ni hayo tu. Hivi sivyo. Kuelekea upande fulani, mashariki au magharibi, sio msingi wa Dini na kupata kheri, lakini kupata wema ni mambo kadhaa wa kadhaa, baadhi yake ni nguzo za itikadi sahihi, na baadhi yake ni katika misingi ya tabia njema na ibada. La kwanza: kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya kufufuliwa na kukusanywa na kuhisabiwa na yatakayo tokea Siku ya Kiyama; na kuamini Malaika, na Vitabu vilivyo teremka kwa Manabii, na kuwaamini wenyewe Manabii. Na pili: kutoa mali kwa kupenda na kuridhia nafsi kuwapa mafakiri katika jamaa, na mayatima, na wenye shida ya haja, na wasafiri walio katikiwa safari yao wasipate cha kuwafikishia wendako, na walio lazimika kuomba kwa haja walio nayo, na kugombo watumwa. (Walio fungwa na kutawaliwa na dhaalimu ni watumwa pia.) Tatu: kushika Sala. Lane: kutoa Zaka iliyo lazimishwa. La tano: kutimiza ahadi kwa hali na mali. La sita: kustahamili maudhi yanayo teremkia roho na mali, mnapo pambana na adui zama za vita. Basi wenye kukusanya imani hizi na vitendo hivi vya kheri ndio walio sadikisha Imani yao, na wao ndio wanao jilinda na ukafiri na mambo machafu na wakayaepuka.

178 Katika Sharia tulizo walazimisha Waumini ni hukumu ya mauwaji ya makusudi. Tumewaandikia kisasi kwa mauwaji. Na wala msichukulie dhulma za kijahiliya, walipo kuwa wakimuuwa muungwana asiye uwa kwa ajili ya mtumwa, na wakimuuwa mwanamume asiye uwa kwa ajili ya mwanamke, na mkuu asiye uwa badala ya mwengine aliyeye uwa, akaachiliwa aliyeye uwa khasa. (Kwa kila ukoo kujiona bora). Yatakikana yule aliyeye uwa auwawe yeye, akiwa ni muungwana, au mtumwa, au mwanamke. Msingi wa sharia ya kisasi ni kuondoa kufanyiana uadui kwa kumuwa yule yule aliyeye uwa ili kuuzima moto wa kulipizana na kuondoa uadui. Walio uliwa mtu wao wakiacha kisasi, wakapendelea kuwasamehe wenzao, watakuwa na haki ya kupewa fidia kwa maiti wao. Na wao inatakikana wawe wasemehevu bila ya kumkahirisha aliyeye uwa. Na juu ya mwenye kuuwa alipe fidia bila ya kujikurupusha. Katika hukumu ya mauwaji kama tulivyo ilazimisha pana wepesi kwa Waumini ukilinganisha na hukumu ya Taurati inayo lazimisha kisasi tu, na kama ilivyo kuwa ni rehema ukilinganisha na watakvavyo wengine kuwa muuwaji aachiliwe bure bila ya kumtaaradhi. Basi mwenye kuivuka hukumu hii baada ya hayo atapata adhabu chungu duniani na Akhera. (Tazama Maelezo 2:178)

179 Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu kwenu ni kubwa kwa hii hukumu ya kisasi. Kwa fadhila ya kisasi jamii yenu ina hakika kupata maisha ya amani na salama. Haya ni kwa kuwa mwenye kutaka kuuwa akijua kuwa naye atauwawa atajizuia kutenda alilo kusudia. Kwa hivyo yeye na yule ambaye angeli uwawa wanahifadhika. Lakini ikiwa kama ilivyo kuwa zama za ujahili akiuliwa mkuu kwa kuuliwa mtu mdogo, na asiye na kosa badala ya mwenye makosa - hapo inakuwa ni kuzua fitna, na kuondoka utulivu na amani. Wenye akili nawazingatie faida ya sharia ya kisasi. Haya yatawapelekea watambue upole wa Mwenyezi Mungu kwao kuendea njia ya uchamngu, na kuzifuata amri za Mwenyezi Mungu *Subhanahu*.

wasia kwa wazazi wake na jamaa zake kwa namna nzuri inayo pendeza. Ni waajibu haya kwa wachamngu.¹⁸⁰

181. Na atakaye ubadilisha wasia baada ya kuusikia, basi dhambi yake ni juu ya wale watakao ubadilisha; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.¹⁸¹

182. Na mwenye kumkhofia muusiaji kwenda kombo au kupata dhambi akasuluhisha baina yao, basi hatakuwa na dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye kurehemu.¹⁸²

183. Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu.¹⁸³

184. (Mfungu) siku maalumu za kuhisabika. Na atakaye kuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimize hisabu katika siku nyengine. Na wale wasio weza, watoe fidiya kwa kumlisha masikini. Na atakaye fanya wema kwa kujitolea, basi ni bora kwake. Na mkifunga ni bora kwenu, kama mnajua.¹⁸⁴

185. Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi. Basi ataye kuwa mjini katika mwezi huu naafunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu katika siku nyengine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hisabu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu

180 Kama tulivyo weka sharia ya kisasi kwa maslaha ya umma na kuhifadhi jamii, vile vile tumeleta sharia ya maslaha ya ukoo na kuulinda, nayo ni Sharia ya Wasiya. Basi mwenye kuona kuwa amekabiliwa na mauti naye akawa na mali basi yatatikana awawekee katika mali yake fungu la wazazi wake na jamaa zake, wale jamaa ambao hawamrithi. Katika hayo afuate mwendo unao pendeza na unakubaliwa na wenye akili. Asiwe akampa tajiri na akamwacha fakiri, bali amfadhilishwe yule mwenye haja zaidi, wala asiweke sawa ila wale wenye pato sawa. Na faridha hiyo ni haki iliyo mwajibikia mwenye kupenda uchamngu na kufuata amri za Dini.

181 Ukitoka wasiya basi huo ni haki iliyo waajibu, haijuzu kuugeza na kuubadilisha ila ikiwa wasiya huo umeacha uadilifu. Mwenye kubadilisha haki akageuza wasiya muadilifu ulio sawa baada ya kujua hukumu hii basi huyo amepanda madhambi yatakayo mletea adhabu. Mwenye kuusia hana kosa kwa yatakayo tokea baada yake, wala hakudhani kuwa atakuwapo atakaye fanya hayo, wala yeye hapatilizwi kwa hayo. Mwenyezi Mungu, hakika, ni Mwenye kusikia na kujua, wala hapana linalo fichikana kwake.

182 Ama ikiwa wasiya umeacha haki na njia iliyo sawa tuliyo kwisha ibainisha, kwa mwenye kufanya wasiya kumharimisha fakiri akampa tajiri, akawawacha jamaa zake akawapa mafakiri wasio rithi watu mbali, basi mwenye kwenda mwendo wa kheri akamrejeza mwenye kufanya wasiya ende sawa, basi hapana dhambi kwa kuugeza wasiya kwa namna hiyo. Na Mwenyezi Mungu hamchukulii kitu kwa hayo, kwani Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mwenye kurehemu.

183 Na kama tulivyo kuwekeeni sharia za Kisasi na Wasiya kwa ajili ya maslaha ya jamii zenu, na kuhifadhi mambo ya ukoo, kadhaalika tumeweka sharia za Saumu ili kuzitengeneza nafsi zenu, ziweze kujikinga na matamano, na kukutukuzeni kuliko wanyama walio baki wanao fuata hisiya za matamano yao tu. Na huku kufaridhishwa Saumu ni kama walivyo faridhishwa kaumu zilizo tangulia. Basi msilione kuwa ni jambo zito mno hili, kwani watu wote walilazimishwa haya. Kulazimishwa Saumu ni kwa ajili ipate kuleleka roho ya uchamngu, na ili muwe watu madhubuti, na nafsi zenu ziongoke sawa.

184 Mameamrisha mfungu siku chache za kuhisabika, na lau Mwenyezi Mungu angependa angeli kufanyieni muda mrefu. Wala hatukulazimishini katika Saumu jambo msilo liweza. Aliye mgonjwa wa maradhi yanayo dhuriana na kufunga, au aliomo safarini, basi anaweza kula na alipe akisha pona au akirejea safarini. Ama asiyekuwa mgonjwa wala si msafiri, lakini hawezi kufunga ila kwa taabu kwa sababu ya udhuru kama ukongwe, na maradhi yasiyo tarajiwa kupona, yeye pia anaweza kula, na juu yake amlishe masikini ambaye hamiliki hata chakula cha siku moja yake. Na mwenye kujitolea kwa ridha yake kufunga zaidi kuliko faradhi itakuwa ni bora zaidi kwake. Kwani Saumu daima ni bora kwa mwenye kujua ukweli wa ibada.

kwa kuwa amekuongoeni ili mpate kushukuru.¹⁸⁵

186. Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka.¹⁸⁶

187. Mmehalalishiwa usiku wa Saumu kuingiliana na wake zenu. Wao ni vazi kwenu, na nyinyi ni vazi kwao. Mwenyezi Mungu anajua kwamba mlikuwa mkizikhini nafsi zenu. Kwa hivyo amekukubalieni toba yenu na amekusameheni. Basi sasa changanyikeni nao na takeni aliyo kuandikieni Mwenyezi Mungu. Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku. Wala msichanganyike nao, na hali mnakaa Itikafu msikitini. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi msiikaribie. Namna hivi Mwenyezi Mungu anabainisha Ishara zake kwa watu ili wapate kumcha.¹⁸⁷

188. Wala msiliane mali zenu kwa baat'ili na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua.¹⁸⁸

189. Wanakuuliza khabarai ya miezi. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya

185 Na siku hizi ni za mwezi wa Ramadhani mwezi wenye daraja tukufu kwa Mwenyezi Mungu ndipo ilipo teremshwa Qur'ani ili kuwaongoa watu wote kwa hoja zake zilizo wazi zinazo fikishia kheri, na zenye kutenga baina ya Haki na baat'ili kwa nyakati zote na vizazi vyote. Basi mwenye kuuwahi mwezi huu naye ni mzima, si mgonjwa, yupo mjini si msafiri, yampasa afunge Saumu. Na aliye mgonjwa anaye dhurika kwa kufunga au alioko safarini anaweza kula, na juu yake kuzilipa zile siku alizo kula kwa kufunga utapo ondoka udhuru. Kwani Mwenyezi Mungu hataki kuwapatisha watu mashaka na taklifa bali Yeye anapenda kuwafanyia watu sahala. Na Mwenyezi Mungu amekubainishieni Mwezi wa Saumu, na amekuongoeni ili mpate kutimiza siku za kufunga, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa uwongofu alio kuongoeni, na akakupeni tawfiki njema. (*Tazama Maelezo 2:185*)

186 Na Mimi nawajua vyema waja wangu, na najua wanayo yafanya na wanayo yawacha. Na Ewe Muhammad! Wakikuuliza waja wangu wakasema: Hivyo Mwenyezi Mungu yupo karibu nasi hata ajue tunayo yaficha na tunayo yatangaza na tunayo yawacha? Waambie: Mimi ni karibu nao zaidi kuliko wanavyo dhani. Na dalili ya hayo ni kuwa ombi la mwenye kuomba linafika wakati huo huo, na Mimi ndiye ninaye pokea hayo maombi wakati huo huo vile vile. Ilivyo kuwa Mimi nimewaitikia maombi yao basi na wao waniitikie Mimi kwa kuamini na kut'ii, kwani hiyo ndiyo njia ya kuongoka kwao na kusibu kwao.

187 Mwenyezi Mungu amekuhalalishieni usiku wa kufunga kuingiana na wake zenu, na wao kuchanganyika nanyi katika maisha na katika malazi. Ilikuwa ni mazito kwenu kujitenga nao, na sasa mmepunguziwa hizo taabu. Mwenyezi Mungu anajua kuwa mlikuwa mkijipunguzia starehe ya nafsi zenu na mkijidhulumu kwa kujizua msiingiane na wake zenu hata usiku wa Ramadhani. Sasa amekusameheni na kukupunguzieni mikazo. Sasa basi msione vibaya kuchanganyika nao, na stareheni kwa aliyo kuhalalishieni Mwenyezi Mungu, na kuleni na mnywe usiku wa Ramadhani mpaka mwone mwangaza wa alfajiri unapo tokeza kutokana na kiza cha usiku. Hapo tena fungeni na mtimize Saumu mpaka linapo kuchwa jua. Na ilivyo kuwa Saumu ni katika ibada zinazo taka mtu kujiepusha na matamano ya roho na kuingiana na wanawake wakati wa mchana, basi kadhaalika katika ibada ya kukaa Itikafu msikitini inahitaji kujitenga na kuacha kustarehe na wake zenu wakati huo mnapo kuwapo katika Itikafu. Na haya ya sharia za Saumu na Itikafu alizo kuwekeeni Mwenyezi Mungu yashikeni baraabara msikaribie kuyavunja. Na Mwenyezi Mungu ameyaweka wazi haya kwa watu kwa namna hii ili wapate kuyaogopa na waepukane na matokeo yake.

188 Mmekatazwa siku zote kula mali ya watu kwa njia isiyo ya haki. Mali ya mtu si halali kwenu ila kwa moja ya njia alizo wekea Sharia Mwenyezi Mungu, kama vile mirathi, au kutunukiwa kwa kupewa na mwenye mali, au kwa mkataba ulio sahihi wenye kuhalalisha kumiliki. Na huenda mmoja wenu hutafuta njia za kumpokonya mwenziwe haki ya mali yake kwa kupeleka kesi mahkamani ili yeye kwa kushirikiana na mahakimu au makadhi na kuleta ushahidi wa uwongo, au uwongo dhaahiri, au kutoa rushwa, wapate kula mali kwa dhulma. Huo ni uovu mno kwa wanao tenda, na malipo yao ni mabaya sana.

watu na Hija. Wala sio wema kuziingia nyumba kwa nyuma. Bali mwema ni mwenye kuchamngu. Na ingieni majumbani kupitia milangoni. Na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.¹⁸⁹

190. Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanza uadui.¹⁹⁰

191. Na wauweni popote mwakutapo, na muwatoe popote walipo kutoeni; kwani fitina ni mbaya zaidi kuliko kuuwa. Wala msipigane nao kwenye Msikiti Mtakatifu mpaka wakupigeni huko. Wakikupigeni huko basi nanyi pia wapigeni. Na hivi ndivyo yalivyo malipo ya makafiri.¹⁹¹

192. Lakini wakiacha basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.¹⁹²

193. Na piganeni nao mpaka pasiwepo fitina, na Dini iwe ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa wenye kudhulumu.¹⁹³

194. Mwezi mtakatifu kwa mwezi mtakatifu. Na vitu vitakatifu vimeekewa kisasi. Anaye kushambulieni nanyi mshambulieni, kwa kadiri alivyo kushambulieni. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wachamngu.¹⁹⁴

189 Na watu wanakuliza khabari za mwezi, unanza mwezi mchanga kama uzi, kisha unakuwa mpaka unatimia kaamili. Tena unapungua mpaka unakuwa kama ulivyo anza. Haukai katika hali moja kama jua. Nini maana ya kugeuka huku hata inakuwa kila siku 29 au 30 unakuja mwezi mpya?

Waambie: Huku kutokea hivi kuandama mwezi na kugeuka yapo ndani yake maslaha ya Dini na dunia pia. Hizi ni alama za kuonyesha nyakati za mambo ya maisha yenu. Zinaonyesha nyakati za Hija, ambayo ni moja katika Nguzo za Dini yenu. Na lau kuwa mwezi ungeli baki namna moja tu kama jua, msingeli tambua nyakati za maisha yenu na Hija zenu. Wala huko kutojua hikima ya kugeuka mwezi kusikupelekeeni kutilia shaka hikima ya Muumba. Wala sio wema kuziingilia nyumba kwa nyuma, kinyume na wafanyavyo watu wote. Lakini wema ni kumchamngu katika nyoyo na kumsafishia niya, na kuziingilia nyumba kwa kupitia milangoni kama wafanyavyo watu wote. Na mtake Haki na dalili iliyo sawa. Basi takeni radhi ya Mwenyezi Mungu, na muio gope adhabu yake na kwa hivyo ndio mtaraji kufanikiwa kwenu, na kufuzu kwenu na kuepuka adhabu ya Moto. (*Tazama Maelezo 2:189*)

190 Na katika kumcha Mwenyezi Mungu ni kustahamili mashaka katika kumt'ii Yeye, na mashaka makubwa kabisa juu ya nafsi ni kuwapiga vita maadui wa Mwenyezi Mungu. Lakini wakikuvamieni, basi piganeni na hao wavamizi. Na mmepewa ruhusa kuurudi uvamizi wao, lakini nyinyi msivamie kwa kuanza nyinyi, au kwa kumuwa asiye kupigeni vita wala hana mahusiano na vita; kwani Mwenyezi Mungu hawapendi wavamizi.

191 Wauweni walio kuanzeni vita popote mnapowakuta, na watoeni Makka, wat'ani wenu ambao wamekulazimisheni kuutoka. Wala msione vibaya, kwani walio kufanyieni nyinyi ni maovu zaidi kuliko kuuwa msikitini, nako ni kuwafitini Waumini katika Dini yao kwa kuwaadhibu huko Makka mpaka wakauacha mji wao kuhifadhi Dini yao. Na huu Msikiti Mtakatifu una utakatifu wake, basi msiuvunje kwa kupigana ndani yake. Lakini wakikupigeni vita ndani yake basi nanyi pia wauweni, na nyinyi kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu, mtashinda. Na malipo ya makafiri ni kufanyiwa wanayo wafanyia watu.

192 Wakirejea wakaacha ukafiri, wakafuata Uislamu basi Uislamu humuitikia anaye ulekea. Na Mwenyezi Mungu atawasamehe ule ukafiri wao wa zamani kwa fadhila yake na rehema yake.

193 Wapigeni vita walio taka kuuweni na kukugeuzeni muache Dini yenu kwa maudhi na mateso mpaka ing'oke mizizi ya fitina na isafike Dini iwe ya Mwenyezi Mungu tu. Wakiuacha ukafiri wao basi wamejiokoa nafsi zao na wataepukana na adhabu. Hapo basi haifai kuwafanyia uadui. Uadui hufanyiwa mwenye kuidhulumu nafsi yake akaiteketeza kwa maasi na akaacha uadilifu kwa maneno na vitendo.

194 Na pindi wakikushambulieni katika mwezi mtukufu msiache kupigana nao, kwani huo ni mtukufu kwao kama ulivyo kuwa mtukufu kwenu. Ikiwa wao watauvunja utukufu wake basi nanyi wakabilini kwa kuzilinda nafsi zenu katika huo mwezi. Na katika mambo matukufu na matakatifu pana sharia ya kisasi na kutendana mfano kwa mfano. Anaye kushambulieni katika matakatifu yenu nanyi jilindeni na uadui huo

195. Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo. Na fanyeni wema. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.¹⁹⁵

196. Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na ikiwa mkizuiwa, basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana. Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike machinjoni mwao. Na atakaye kuwa mgonjwa au ana vya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidiya kwa kufunga au kwa kutoa sadaka au kuchinja wanyama. Na mtakapo kuwa salama, basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama aliye mwepesi kumpata. Na asiye pata, afunge siku tatu katika Hija na siku saba mtakapo rudi; hizi ni kumi kaamili. Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.¹⁹⁶

197. Hija ni miezi maalumu. Na anaye kusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija. Na kheri yoyote mnayo ifanya Mwenyezi Mungu anaijua. Na jitengezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamngu. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili!¹⁹⁷

198. Si vibaya kwenu kuitafuta fadhila ya Mola wenu Mlezi. Na mtakapo miminika kutoka *A'rafat* mtajeni Mwenyezi Mungu penye *Masha'ril Haram*. Na mkumbukeni

kwa mfano wake. Na mcheni Mwenyezi Mungu, msikiuke mipaka katika kulipiza kisasi. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwanusuru wachamngu.

195 Kupambana na makafiri kunahitaji kutoa roho kama ilivyo kutoa mali. Basi toeni kwa kuandaa vita, na jueni kuwa kupigana na hawa ni kupigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Basi msikae tu. Toeni mali kwa ajili yake, kwani mkitofanya na mkafanya ubakhili adui atakupandeni na atakudhilini. Hapo itakuwa kama mlio jitokomeza wenyewe kwenye maangamio. Tendeni lilio kuwajibikieni kwa uzuri na vilivyo, kwani Mwenyezi Mungu hupenda anapo fanya jambo mtu alifanye vizuri. (*Tazama Maelezo 2:195*)

196 Timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa ukamilifu, wala yasiwe makusudio yenu ya kidunia kama kutaka umaarufu na kadhaalika. *Mkiharimia Hija* na *Umra* akakuzuieni adui njiani basi mtatoka katika *Ihram* yenu kwa kunyoa nywele. Lakini kabla ya hayo mchinje mnyama aliye mwepesi kumpata, kama mbuzi au ngamia au ng'ombe, na kumtoa sadaka kwa masikini. Wala msinyoe mpaka mtimize haya. Mwenye kuharimia akapata maudhi katika nywele zake kwa maradhi au wadudu hapana ubaya kunyoa. Juu yake hapo atoe fidiya kwa kufunga siku tatu, au kutoa sadaka kuwalisha masikini sita chakula cha kutwa, au kuchinja mbuzi na kumtoa sadaka kwa masikini. Na ikiwa mpo katika amani na salama na hakukutokeleeni adui njiani, na mkakusudia Hija na Umra, na mkajistarehesha kwa kufanya Umra kwanza mpaka ufike wakati wa Hija ndio mharimie, basi inakupaseni kuchinja mbuzi kwa ajili ya masikini na mafakiri wa Makka. Asiye pata mbuzi au hamiliki bei yake afunge siku tatu hapo Makka, na siku saba akisha rejea kwao. Haya ni kwa aliye kuwa hana watu wake Makka. Kwa mwenye watu wake Makka hapana kitu akijistarehesha.

197 Na Hija inakuwa katika miezi mnayo ijua, kwani jambo hili ni maarufu kwenu tangu zama za Ibrahim a.s. nayo ni miezi ya Mfungo Mosi, Mfungo Pili na Mfungo Tatu. Mwenye kuazimia faridha ya Hija katika miezi hii na akaingia basi afuate vilivyo adabu zake. Katika adabu za Hija ni kuwa mwenye kuharimia ajiepushe na kuingiana na wakeze, na kufanya maasi ya kutukanana na mengineyo, kujadiliana na kubishana na Mahujaji wenziwe, na ajiepushe na kila linalo pelekea chuki na khasama ili atoke katika Ihramu yake naye hali ana hishima yake. Ajitahidi kufanya kheri na kutafuta malipwa kwa Mwenyezi Mungu kwa kutenda mema, kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua hayo na ni Mwenye kulipa vitendo vyema. Na mchukue zawadi za Akhera yenu kwa kuchamngu na kufuata amri za Mwenyezi Mungu na kuyaepuka ayakatazayo. Hiyoy, basi ndio zawadi bora. Na kuweni wenye kuhisi khofu ya Mwenyezi Mungu katika yote mnayo yafanya na mnayo yawacha kwa mujibu wa akili na hikima njema. Katika vitendo vyenu vyote msichanganyishe hata chembe na mambo ya pumbao au makusudio ya kidunia.

kama alivyo kuongoeni, ijapo kuwa zamani mlikuwa miongoni mwa walio potea.¹⁹⁸

199. Kisha miminikeni kutoka pale wanapo miminika watu, na muombeni Mwenyezi Mungu msamaha: hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.¹⁹⁹

200. Na mkisha timiza ibada zenu basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyo kuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi. Na wapo baadhi ya watu wanao sema: Mola wetu Mlezi, tupe duniani! Naye katika Akhera hana sehemu yoyote.²⁰⁰

201. Na katika wao wapo wanao sema: Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na utulinde na adhabu ya Moto!²⁰¹

202. Hao ndio watakao pata sehemu yao kwa sababu ya yale waliyo yachuma. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.²⁰²

203. Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika zile siku zinazo hisabiwa. Lakini mwenye kufanya haraka katika siku mbili (akarejea) si dhambi juu yake; na mwenye kukawia pia si dhambi juu yake, kwa mwenye kumchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba nyinyi mtakusanywa kwake.²⁰³

204. Na katika watu yupo yule ambaye maneno yake kwa maisha ya kidunia

198 Na walikuwako miongoni mwenu ambao wakiona vibaya kufanya biashara na kutafuta riziki wakati wa msimu wa Hija. Basi mnaambiwa kuwa hapana ubaya kwenu hayo, bali mnaweza kuchuma maisha kwa njia ziliyo ruhusiwa na sharia, na mtafute fadhila na neema za Mwenyezi Mungu. Wakitoka Mahujaji A'rafat baada ya kusimama huko, na wakafika *Muzdalifa* katika mkasha wa Idi ya Kuchinja, wamtaje Mwenyezi Mungu hapo *Masha'ril Haram*, napo ndipo kwenye kilima cha *Muzdalifa*, kwa kusoma *Tahlili* na kuitikia *Labbaik* na kusoma *Takbir*. Na wamtukuze Mwenyezi Mungu wakimhimidi na kumshukuru kwa vile alivyo waongoa kwenye Dini ya Haki na ibada iliyo nyooka katika *Hija* na *Umra*, na ilhali kabla ya hapo walikuwa katika walio potea njia ya uwongofu.

199 Makureshi walikuwa hawasimami na watu wengine katika A'rafat juu ya kuwa wakijua kuwa baba yao Ibrahim akisimama hapo. Na hayo ni kwa kujitukuza wasiwe sawa na wengineo na hali wao ati ni watu wa Nyumba ya Mwenyezi Mungu na ni wakaazi wa katika pahala patakatifu. Wakidai kuwa hayo ni kuitukuza Makka wasitoke kwenda A'rafat ambako si kutakatifu kama Makka. Mwenyezi Mungu akawalazimisha wazing'olee mbali hizo ada za kijinga, na wasimame katika A'rafat, na watoke huko kama watokavyo watu wote. Kwani hapana yeyote aliye bora kuliko mwengine katika utendaji wa ibada. Na inawapasa wamwombe Mwenyezi Mungu maghfira katika mwahala humu mwenye baraka. Hayo ndiyo yana maelekeo zaidi Mwenyezi Mungu kuwasamehe dhambi na makosa yao, na akawarehemu kwa fadhila yake.

200 Mkisha maliza a'mali za Hija na ibada zake wacheni mliyo kuwa mkiyafanya zama za ujahili ya kutafakhari kwa baba zenu na kukumbusha mambo yao, bali makumbusho yenu na kutukuza kwenu kuwe kwa Mwenyezi Mungu kama mlivyo kuwa mkiwakumbuka baba zenu, bali mtajeni Yeye kwa wingi zaidi kuliko wazee wenu, kwani Yeye ndiye Mwenye kuzitawala neema zenu na neema za baba zenu vile vile. Na humu mwahali mwa Hija ndio khasa mwahala mwa dua na kuombea fadhila na kheri na rehema zitokazo kwa Mwenyezi Mungu. Na walikuwako baadhi ya Mahujaji wakifupiza dua zao kwa mambo na kheri za dunia tu. Hao hawapati sehemu yoyote ya Akhera.

201 Na wapo watu ambao Mwenyezi Mungu amewawezesha nyoyo zao zikapelekea kuomba kheri ya dunia na Akhera, na wakamwomba Mwenyezi Mungu awaepushe na shari na adhabu ya Moto.

202 Hawa wanapewa kama walivyo jaaliwa kuyachuma kwa kumwomba na kumtegemea Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu humlipa kila mtu kama anavyo stahiki, na ni Mwepesi wa kuhisabu na kulipa.

203 Na mtajeni Mwenyezi Mungu kwa Takbiri na vinginevyo katika siku maalumu, nazo ni siku za kutupa mawe hapo Mina, nazo ni taarikh 11 na 12 na 13. Na si lazima kwa Haji kukaa siku tatu hizi Mina akitupa mawe, bali anaweza kufupiza siku mbili, kwani msimamo wa kheri ni kuchamngu, si idadi. Na daima mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kuwa kwake Yeye mtakusanywa na muulizwe mliyo yatenda. (*Tazama Maelezo 2:203*).

hukufurahisha; naye humshuhudisha Mwenyezi Mungu kwa yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye ndiye mkubwa wa ukhasimu.²⁰⁴

205. Na anapo tawala hufanya juhudi katika nchi kwa kufisidi humo na kuteketeza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu hapendi ufisadi.²⁰⁵

206. Na akiambiwa: Mwoope Mwenyezi Mungu, hupandwa na mori wa kutenda madhambi. Basi huyo inamtosha Jahannam. Paovu mno hapo kwa mapumziko.²⁰⁶

207. Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake.²⁰⁷

208. Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu, wala msifuate nyayo za She'tani; hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi.²⁰⁸

209. Na ikiwa mkateleza baada ya kukufikieni hoja zilizo wazi, basi jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.²⁰⁹

210. Je wanangoja mpaka Mwenyezi Mungu awajie katika vivuli vya mawingu pamoja na Malaika, na hukumu iwe imekwisha tolewa? Na kwa Mwenyezi Mungu ndio hurejeshwa mashauri yote.²¹⁰

211. Waulize Wana wa Israili: Tumewapa ishara ngapi zilizo wazi? Na anaye zibadili neema za Mwenyezi Mungu baada ya kumfikia basi hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.²¹¹

204 . Ilivyo kuwa kumcha Mwenyezi Mungu ndio msingi, basi khasara ni ya wale watu ambao dhamiri walio nayo nyoyoni mwao ni mbali na maneno yanayo tamkwa na ndimi zao. Wamepewa utamu wa kupanga maneno, hukufurahisha kauli yao katika kujivutia manufaa ya maisha ya kidunia, na kuunga mkono kwa wayasemayo humsingizia Mwenyezi Mungu kuwa anashuhudia kuwa wayasemayo yanatoka nyoyoni mwao. Kumbwao kwa hakika ndio wakubwa wa ukhasama na ukhabithi kwako wewe.

205 Na pindi wakitawalisha madaraka yoyote haiwi juhudi yao kuleta maslaha, bali ni kuleta ufisadi na kuteketeza mimea, kukata miti na kuuwa wanyama na binaadamu. Na Mwenyezi hawapendi watu kama hawa, kwani Mwenyezi Mtukufu hapendi uharibifu.

206 Akinasihiwa amwoope Mwenyezi Mungu huzidi kupanda mori wake na akadhani kuwa hivyo unamvunjia cheo chake, akazidi kupanda madhambi na kuzidi kumchafua na kumwongeza inadi. Mtu huyo hatoshelezeki mpaka aingie Jahannam, na hayo ni makao maovu mno.

207 Ni farka kubwa baina ya wanaofiki hawa na Waumini wa kweli ambao watayari kuza nafsi zao kwa sababu ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na kulitukuza Neno la Haki. Hawa ni kinyume na wale wa kwanza. Hawa wakitawalisha madaraka kuendesha mambo ya watu inakuwa ni katika upole wa Mwenyezi Mungu kuwafanya waja wake. Mwenyezi Mungu Mtukufu huwarehemu hao waja wema kwa kuwatawalisha watu wema ili awalinde na wenyewe shari.

208 Enyi mlio amini! Na iwe baina yenu nyote amani na salama, wala msichochee chuki za kijahiliya na mengineyo kuleta sababu za ugomvi na khitilafu. Wala msipite katika njia ya Shetani anaye kupelekeeni kugawanyika, kwani yeye ni adui wenu aliye dhaahiri. (*Tazama Maelezo 2:208*)

209 Mkiageuka mkaicha Njia hii mliyo itiwia muifuate nyote baada ya kudhahiri hoja za kukata kuwa ndiyo Njia ya Haki, basi jueni mpatilizwa kwa kugeuka huko, kwani Mwenyezi Mungu hakika ni Mwenye nguvu, humuadhibu mwenye kuiacha Njia yake, na Mwenye hikima anaye pima kadiri ya adhabu yake.

210 Je, hao wanao ukataa Uislamu wanangojea mpaka wamwone Mwenyezi Mungu Mtukufu na Malaika jahara katika mawingu na hukumu ya kuwakatisha tamaa zao imekwisha pitishwa? Kwani hakika mambo yote yamo mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Yeye huyasarifu atakavyo, na hukumu yake imekwisha tolewa, na hapana shaka yoyote itatekelezwa tu.

211 Waulize Wana wa Israili tumewaletea dalili ngapi za kukata za kuthibitisha ukweli wa Mtume! Na hayo ni neema ya kutaka kuwaongoa wamwendee Mwenyezi Mungu. Lakini wapi! Walizikataa hizo dalili na wakashikilia kuzikanusha hadi ya kuyageuza makusudio yake. Baada ya kuwa hizo dalili ni kwa ajili ya uwongofu zikawa kwa ukafiri wao ni sababu ya kuwazidisha upotovu na kutenda dhambi. Na mwenye kugeuza neema ya Mwenyezi Mungu kwa namna hii basi huyo anastahiki adhabu, na Mwenyezi

212. Walio kufuru wamepambiwa maisha ya duniani; na wanawafanyia maskhara walio amini. Na wenye kuchamngu watakuwa juu yao Siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.²¹²

213. Watu wote walikuwa ni umma mmoja. Mwenyezi Mungu akapeleka Manabii wabashiri na waonyaji. Na pamoja nao akateremsha Kitabu kwa Haki, ili kihukumu baina ya watu katika yale walio khitalifiana. Na wala hawakukhitalifiana ila wale walio pewa Kitabu hicho baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, kwa sababu ya uhasidi baina yao. Ndipo Mwenyezi Mungu kwa idhini yake akawaongoa walio amini kwendea haki katika mambo waliyo khitalifiana. Na Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye kwenye Njia Iliyo Nyooka.²¹³

214. Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, bila ya kukujieni kama yaliyo wajia wale walio pita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara na wakatikiswa hata Mtume na walio amini pamoja naye wakasema: Lini nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja? Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu.²¹⁴

215. Wanakuuliza watoe nini? Sema: Kheri mnayo itoa ni kwa ajili ya wazazi na jamaa na mayatima na masikini na wasafiri. Na kheri yoyote mnayo ifanya Mwenyezi Mungu anaijua.²¹⁵

216. Mmeandikiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui.²¹⁶

Mungu hakika ni mkali wa kuadhibu.

212 Na sababu ya kupotoka na kukufuru ni kuitaka dunia. Wale walio kufuru wamepambiwa matamanio ya maisha ya kidunia wakawa wanawakejeli wale walio amini kwa kushughulikia kwao maisha ya Akhera. Na Mwenyezi Mungu atawaweka walio amini pahala pa juu kabisa kuliko wao katika Akhera. Ama kuwa hawa makafiri wana mali zaidi na mapambo ya kidunia hakuonyeshi ubora wao, kwani riziki ya Mwenyezi Mungu haipimwi kwa mujibu wa kuamini na kukufuru, bali inakwenda kama apendavyo Yeye mwenyewe. Wapo watu huzidishiwa hiyo riziki kwa "Istidraaji" kumpururia kamba tu, na wapo wanao nyimwa neema za dunia kama ni mtihani, majaribio.

213 Hakika watu wana tabia moja ya kuwa wapo tayari kupotoka, na wapo ambao sababu za uwongofu zinakuwa na nguvu kwao, na wengine upotovu ndio unawatawala. Kwa hivyo wakakhitalifiana. Mwenyezi Mungu akawapeleka Manabii kuwaongoa na kuwabashiria kheri na kuwaonya. Na akateremsha kwa hao Manabii Vitabu vyenye kukusanya Haki, ili viwe ndivyo vya kuwahukumu iondoke mizozo baina yao. Lakini wale walio nafika na uwongofu wa Manabii ndio wao tu walio amini, hao ambao Mwenyezi Mungu amewaongoa kutokana na khitilafu wakafuata Haki. Na Mwenyezi Mungu ndiye anaye wapa tawfiqi watu wa Haki pindi wakisafi niya zao.

214 Hivyo mnadhani kuwa mtaingia Peponi kwa Uislamu wa kutamka tu bila ya kupatikana na masaibu mfano wa masaibu yaliyo wasibu walio kuwa kabla yenu? Hao walipata shida na mashaka na mateso, wakatikiswa mpaka ikafika hadi ya kuwa Mtume wao mwenyewe kusema, na wao wakasema vile vile pamoja naye: Lini itakuja nusura ya Mwenyezi Mungu? Mola wao Mlezi basi anawahakikishia kwa ahadi yake kwa kuwajibu kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu.

215 Waumini wanakuuliza mas-ala ya kutoa. Waambie: Kutoa iwe kutokana na mali mazuri, na wa kupewa ni wazazi wawili, na jamaa, na mayatima, na masikini, na msafiri aliye katikiwa na mali yake na watu wake. Na lolote katika vitendo vya kheri mlitendalo basi hakika Mwenyezi Mungu analijua na atakulipeni kwalo.

216 Ikiwa kutoa kusaidia mayatima na masikini na wengineo ni kuhami jamii ya umma kwa ndani, kadhaalika kupigana vita ni kuhami umma na adui wa nje. Kwa hivyo enyi Waislamu, mmelazimishwa kupigana vita kuhami Dini yenu, na kulinda nafsi zenu. Hakika hizo nafsi zenu kwa mujibu wa tabia zake zinachukia mno kupigana. Lakini huenda mkachukia kitu na ndani yake ipo kheri kwenu, na mkapenda kitu na ikawa ipo shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anayajua maslaha yenu ambayo yamefichikana, na nyinyi hamyajui. Basi tendeni mlilo amrisha kulitenda.

217. Wanakuuliza juu ya kupigana vita katika mwezi mtakatifu. Sema: Kupigana vita wakati huo ni dhambi kubwa. Lakini kuzuilia watu wasende katika Njia ya Mwenyezi Mungu na kumkanusha Yeye, na kuzuilia watu wasende kwenye Msikiti Mtakatifu na kuwatoa watu wake humo, ni makubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na fitina ni mbaya zaidi kuliko kuuwa. Wala hawatoacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika Dini yenu kama wakiweza. Na yeyote katika nyinyi akiacha Dini yake akafa naye ni kafiri, basi hao ndio ambao a'mali zao zimeharibika duniani na Akhera. Na hao ndio watu wa Motoni; humo watadumu.²¹⁷

218. Hakika wale walio amini na wale walio hama na wakapigania Njia ya Mwenyezi Mungu, hao ndio wanao taraji rehema za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.²¹⁸

219. Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa na manufaa kwa watu. Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake. Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Kileo chepesi. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake mpate kufikiri--²¹⁹

220. --katika mambo ya dunia na mambo ya Akhera. Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: Kuwatengeneza ndio kheri. Na mkichanganyika nao basi ni ndugu zenu; na Mwenyezi Mungu anamjua mharibifu na mtengenezaji. Na Mwenyezi Mungu angeli penda angeli kutieni katika udhia. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.²²⁰

217 Waislamu walichukia kupigana katika mwezi mtakatifu, ndio wakakuuliza juu yake. Waambie: Naam, kupigana katika mwezi mtakatifu ni dhambi kubwa. Lakini kubwa zaidi ni haya wayatendayo maadui zenu nayo: kuwazuia watu wasifuata Njia ya Mwenyezi Mungu, wasende kwenye Msikiti Mtakatifu, na kuwafukuza Waislamu kutoka Makka. Na hayo maudhi na mateso yao kuwafanyia Waislamu ili waache Dini yao ni makubwa zaidi kuliko mauwaji yoyote. Kwa hivyo imehalalishwa kupigana vita katika mwezi mtakatifu kwa ajili ya kupambana na maovu haya. Hichi ni kitendo kikubwa cha kujikinga na lilio kubwa zaidi. Enyi Waislamu! Jueni kuwa mwendo wa watu hawa ni mwendo wa ukhalifu na udhaalimu. Na wao hawakubali kwenu uadilifu wala mambo ya kiakili. Na wala hawatasita kukupigeni vita mpaka wakuachisheni Dini yenu pindi wakiweza. Na atakaye dhoofika kwa mashambulio yao akaacha Dini yake na akafa katika ukafiri, basi watu kama hao watapoteza vitendo vyao vyema vyote vya duniani na Akhera. Na hao ni watu wa Motoni ambako watadumu.

218 Wenye kuamini imani ya kweli hata wakahama kwa ajili ya kuinusuru Dini na kwa ajili ya Jihadi ili Dini ienee hao wanangojea thawabu kubwa za Mwenyezi Mungu. Na ikiwa wamefanya kasoro kitu basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, anasamehe dhambi, Mwenye kurehemu, anawarehemu waja wake kwa uwongofu na kuwalipa.

219 Ewe Muhammad! Wanakuuliza juu ya hukumu ya ulevi na kamari. Waambie kwamba katika yote mawili hayo pana madhara makubwa, kwa kuharibu siha na kupoteza akili na mali, na kuleta chuki na uadui baina ya watu. Pia ndani ya hayo yapo manufaa, kama kujipumbaza na kupata faida ya sahali. Lakini madhara yake ni makubwa zaidi kuliko manufaa yake, basi epukaneni nayo. Na wanakuuliza watoe nini? Wajibu watoe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kileo chepesi na hakina uzito kukitoa. Hivyo ndio Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake mpate kufikiri yale yatakayo kurejeeni katika maslaha ya dunia na Akhera. (*Tazama Maelezo 2:219*)

220 Na wanakuuliza khabari ya mayatima: katika Uislamu inapasa watendejwe? Sema ni kheri yenu na yao kuwatendea wema. Wawekeneni katika nyumba zenu pamoja nanyi, na changanyikeni nao kwa makusudio ya kheri si ya fisadi, kwani wao ni ndugu zenu duniani, wanahitaji kwenu mchanganyiko huu. Na Mwenyezi Mungu anamjua mharibifu na mtengenezaji katika nyinyi. Basi tahadharini! Na Mwenyezi Mungu angeli penda angeli kupeni taabu, akakulazimisheni kuwaangalia mayatima bila ya kuchanganyika nao, au angeli kuacheni bila ya kubainisha waajibu wanao pasa kutendewa. Kwa hivyo wangelikulia kuchukia watu, na hayo yange pelekea kufisidika na kuleta shida kwa jamii zenu.

221. Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini. Na mjakazi Muumini ni bora kuliko mshirikina hata akikupendezeni. Wala msiwaoze (binti zenu) wanaume washirikina mpaka waamini. Na mtumwa mwanamume Muumini ni bora kuliko mshirikina hata akikupendezeni. Hao wanaitia kwenye Moto, na Mwenyezi Mungu anaitia kwenye Pepo na maghafira kwa idhini yake. Naye huzibainisha Aya zake kwa watu ili wapate kukumbuka.²²¹

222. Na wanakuuliza juu ya hedhi. Waambie, huo ni uchafu. Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi. Wala msiwaingilie mpaka wat'ahirike. Wakisha t'ahirika basi waendeeni alivyo kuamrishi Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao tubu na huwapenda wanao jisafisha.²²²

223. Wake zenu ni kama konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo. Lakini jitangulizieni kheri nafsi zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kuwa hakika nyinyi mtakutana naye. Na wape bishara njema Waumini.²²³

224. Wala msifanye jina la Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu kuwa ni kisingizio cha kuacha kufanya wema na kuchamngu na kupatanisha baina ya watu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua.²²⁴

225. Mwenyezi Mungu hakushikeni kwa viapo vyenu vya upuuzi. Bali anakushikeni kwa yanayo chuma nyoyo zenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mpole.²²⁵

Kwani kuwakahirisha mayatima na kuwadhili huwafanya wawachukie hao jamaa wawatendao vibaya. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda katika amri yake, lakini naye ni Mwenye hikima halazimishi katika sharia ila lenye maslahu yenu.

221 Hapana ubaya wowote kuchanganyika na mayatima, lakini kuchanganyika na washirikina ni vibaya. Muumini hana ruhusa kumwoa mshirikina asiye fuata dini ya Kitabu cha mbinguni. Basi msipelekwewa kutaka kumwoa mwanamke wa kishirikina kwa ajili ya mali yake, au uzuri wake, au jaha yake, au ukoo wake. Muumini aliye mtumwa ni bora kuliko mshirikina aliye huru mwenye mali, na jamali, na utukufu na nasaba. Wala nyinyi msiwaoeze wanawake walio mikononi mwenu wanaume wa kishirikina wasio amini Vitabu vya mbinguni, wala yasikupelekeeni kumkhiari mshirikina utajiri na cheo chake. Mtumwa Muumini ni bora kuliko huyo. Hao washirikina wanawavutia wenzao kwenda katika maasi na ushirikina, na kwa hivyo wanapaswa kuingia Motoni. Na Mwenyezi Mungu anapo kulinganieni mjitenge na ndoa za washirikina anakulinganieni kwa ajili ya maslahu yenu na mwongoke ili mpate Pepo na maghfira, na mwende katika njia ya kheri kwa taisiri. Na Mwenyezi Mungu anabainisha sharia zake na uwongofu wake kwa watu wapate kujua maslahu yao na kheri yao.

222 Na wanakuuliza juu ya kuwaingilia wake zenu wakati wanapo kuwa na damu ya mwezi, hedhi. Waambie kuwa hedhi ni uchafu. Basi jizuieni kuwaingilia wakati wake mpaka wat'ahirike (wasafike). Wakit'ahirika basi ingianeni nao katika njia za maumbile. Na ikiwa mtu amefanya makosa katika haya, basi na atubu, na Mwenyezi Mungu anapenda waja wake wakithiri toba na usafi kutokana na uchafu. (Tazama Maelezo 2:222)

223 Wake zenu ni mwahali mwa kupatia uzazi, kama vile mbegu inavyo toa mmea. Basi ni halali kwenu kuwaingilia vyovyote kwa sharti ya kupitia njia za uzazi. Na mcheni Mwenyezi Mungu wala msimuasi katika kukaa kwenu na wanawake. Na mjue kuwa nyinyi mtakutana naye, na mna jukumu kwake. Furaha ni ya hao wanao simama juu ya mipaka yake Mtukufu na hawaikiuki.

224 Msilichezee jina la Mwenyezi Mungu katika kukithirisha viapo, kwani hivyo inakuwa ni kinyume na kulitukuza jina la Mwenyezi Mungu. Na hakika kujilinda na kukithirisha kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ndio hupelekea vitendo vyema, na kuchamngu, na kuweza kusuluhisha baina ya watu. Mwenye kujilinda hivyo huwa anatukuka cheo katika macho ya watu, na anakuwa anaaminika, na kauli yake hukubalika kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia maneno yenu na yamini zenu, na Mjuzi wa niya zenu.

225 Mwenyezi Mungu amekusameheni baadhi ya yamini zenu. Lilio mpitia mtu ulimini mwake katika viapo bila ya kukusudia wala kulitia moyoni, au akaapa kwa kuamini kuwa limetukia na halikutukia,

- 226.** Kwa wanao apa kuwa watajitenga na wake zao, wangojee miezi mine. Wakirejea basi Mwenyezi Mungu hakika ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.²²⁶
- 227.** Na wakiazimia kuwapa talaka basi, Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mjuzi.²²⁷
- 228.** Na wanawake walio achwa wangoje peke yao mpaka t'ahara (au hedhi) tatu zipite. Wala haiwajuzii kuficha alichu umba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, ikiwa wanamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na waume wao wana haki ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka kufanya sulhu. Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao. Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.²²⁸
- 229.** T'alaka ni mara mbili. Kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa vizuri. Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichu wapa wake zenu, ila ikiwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kuwa hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu hapo itakuwa hapana lawama ikiwa mwanamke atajikomboa. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiikiuke. Na watakao ikiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu, hao ndio madhaalimu.²²⁹
- 230.** Na kama amempa t'alaka (ya tatu) basi si halali kwake baada ya hayo mpaka aolewe na mume mwengine. Na akiachwa basi hapana ubaya kwao kurejeana wakiona kuwa watashikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu anayo ibainisha kwa watu wanao jua.²³⁰

Mwenyezi Mungu hayachukuli hayo. Lakini anakushikeni kwa mnayo yaazimia katika nyoyo zenu kuwa yamekuwa au hayakuwa, na kwa kusema uwongo pamoja na kuuwapia yamini. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kumghufiria mwenye kutubu, ni Mpole, anasamehe lisilo kusudiwa moyoni.

226 Na hawa walio apa kuwa hawatawakaribia wake zao, na wangoje muda wa miezi mine. Wakiwaingilia wake zao mnamo muda huu ndoa itaendelea, lakini juu yao ni kafara kwa yamini yao. Na Mwenyezi Mungu amewasamehe na anakubali kafara kwa rehema yake kuwahurumia.

227 Na ikiwa hawakuwaingilia wake zao katika muda huu inakuwa hayo ni madhara kwa mwanamke. Basi hapana ila t'alaka tu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuzisikia yamini zao, na Mwenye kujijua hali zao, na atawahisabu kwa hayo Siku ya Kiyama.

228 Yawapasa wat'alaka wangojee bila ya kufanya pupa ya kuolewa muda wa hedhi tatu, ili kuhakikisha hawana mimba na kujipa nafasi ya kumkinika kurejeana. Wala si halali kwao kuficha mimba au damu ya hedhi. Huo ndio mwendo wa wanawake wanao muamini Mwenyezi Mungu na kukutana naye Siku ya Akhera. Na waume zao wanayo haki kuwarejea katika ule muda wa eda. Na wanaume wanapo tumia haki wakusudie kupatana si kudhuru. Wanawake nao wana haki mfano wa jukumu lilio juu yao katika mambo yasio kuwa kinyume na Sharia Tukufu. Na wanaume wana daraja juu yao ya ulinzi na kuyahifadhi maisha ya nyumbani na mambo ya watoto. Mwenyezi Mungu *Subhanahu* yuko juu ya waja wake, na Yeye ndiye anawatungia sharia zinazo wafikiana na hikima. (*Tazama* Maelezo 2:228).

229 T'alaka ni mara mbili. Baada ya kila t'alaka ana haki mume kukaa naye kwa kumrejea kabla ya kwisha siku za eda, au kumrejesha katika dhamana yake kwa kumwoa upya. Na katika hali hiyo inapasa makusudio yake ni kukaa naye kwa uadilifu na kumtendea wema, au kuachana kwa ihsani na heshima bila ya kukhasimiana. Wala si halali kwenu, enyi waume, kuchukua chochote mlichu wapa wanawake ila mkikhofu kuwa hamtoweza kufuata haki za uke na ume alizo kubainishieni Mwenyezi Mungu *Subhanahu* wa Taa'la, na akaku lazimisheni mzifuate. Mkikhofu, enyi Waislamu, kutofuata haki za mume na mke vilivyo kama alivyo eleza Mwenyezi Mungu basi ameamrisha mke atoe mali kwa ajili ya kutokana na mumewe. Na hizi ni hukumu zilizo pitishwa, msiende kinyume nazo, mkazipindukia. Mwenye kufanya hivyo amejidhulumu nafsi yake na amedhulumu jamii anayo ishi kati yake. (*Tazama* Maelezo 2:229)

230 Mume akimwacha mkewe mara ya tatu baada ya t'alaka mbili za mwanzo basi hamhalalikii mpaka yule mke aolewe na mume mwengine aingie harus. Akimwacha baada ya hapo basi anaweza kufunga

231. Na mtakapo wapa wanawake t'alaka, nao wakafikia kumaliza eda yao, basi warejeeni kwa wema au waachilieni kwa wema. Wala msiwarejee kwa kuwadhuru mkafanya uadui. Na atakaye fanya hivyo, amejidhulumu nafsi yake. Wala msizichukulie Aya za Mwenyezi Mungu kwa maskhara. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu, na aliyo kuteremshieni katika Kitabu na hikima anacho kuonyeni kwacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.²³¹

232. Na mtakapo wapa wanawake t'alaka nao wakamaliza eda yao, basi msiwazuie kuolewa na waume zao endapo baina yao wamepatana kwa wema. Hayo anaonywa nayo yule miongoni mwenu anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ni bora zaidi kwenu na safi kabisa. Na Mwenyezi Mungu anajua, lakini nyinyi hamjui.²³²

233. Na wazazi wanawake wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kaamili kwa anaye taka kutimiza kunyonyesha. Na juu ya baba yake chakula cha kina mama, na nguo zao kwa mujibu wa ada. Wala halazimishwi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Mama asitiwe taabuni kwa ajili ya mwanawe, wala baba kwa ajili ya mwanawe. Na juu ya mrithi mfano wa hivyo. Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa kwa kuridhiana na kushauriana, basi si vibaya kwao. Na mkitaka kuwapatia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha basi hapana ubaya kwenu mkitoa mlichu ahidi kwa mujibu wa ada. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayo yatenda.²³³

ndoa tena na yule mume wa kwanza, na wala hapana dhambi juu yao kuanza maisha mapya kwa ndoa mpya. Lakini yawapasa waazimie kuendesha maisha mema ya mume na mke wakifuata sharia alizo ziweka mipaka Mwenyezi Mungu *Subhanahu* wa Taa'la. Na mipaka hii imebainishwa wazi kwa mwenye kuamini sharia ya Kiislamu na anataka ilimu na a'mali njema.

231 Mnapo wawacha wake wakakaribia kumaliza eda zao mnaweza kuwarejea kwa makusudio ya uadilifu na kukaa nao kwa wema bila ya kuwadhuru, na pia mnaweza kuwaacha watimize eda zao kwa kuzingatia muamala mwema ulio laiki wakati wa kufarikiana bila ya kuwatendea mabaya. Wala haijuzu katika kuwarejea ikawa makusudio yake ni madhara na kuirefusha eda. Mwenye kutenda hayo basi mwenyewe amejinyima starehe ya maisha ya mke na mume, na imani ya watu kwake, na anastahiki kukasirikiwa na Mwenyezi Mungu. Wala msizifanyie maskhara na mchezo na kuwa ni upuuzi hukumu za Mwenyezi Mungu zilizo kuja katika Aya hizi kwa ajili ya kutengeza maisha ya kinyumba, na zikaweka *khatamu* za ukoo katika mikono ya wakili, naye ni mume, mkawa mnatoa t'alaka bila ya sababu, na mkawapatisha wake zenu madhara na maudhi. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu kwa kukupangieni mpango bora kabisa katika maisha ya ndoa, na pia kwa aliyo kuteremshieni katika Kitabu kilicho bainisha wazi ujumbe wa Muhammad, na ilimu mbali mbali zenye manufaa, na mifano na hadithi za kukuwaidhini na kukuongoeni. Na jikingeni na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Jueni kuwa Mwenyezi Mungu anajua siri zenu na mnayo dhihirisha na niya zenu na vitendo vyenu. Naye ni Mwenye kukulipeni kwa myatendayo.

232 Mnapo waacha wake na zikatimia eda na akitaka mwanamke kuanza maisha mapya kwa kuolewa tena ama na yule mku-mwenziwe au na mwanamume mwengine, basi si halali kwa wazee wala yule mku-mwenza kuwakataza, ikiwa pande mbili zimeridhiana kufanya ndoa mpya kwa kutaka maisha bora yatakayo pelekea masikilizano mema baina yao. Anawaidhiwa hayo anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Mwendu huo unapelekea kukuza mahusiano ya hishima na sharaf katika jamii zenu, na ni usafi zaidi katika nafsi zenu kut'ahirika na uchafu na mahusiano yaliyo maovu. Na Mwenyezi Mungu anajua maslahi ya binaadamu na siri za nafsi zao ambazo wao hawajui vipi kuzipata.

233 Ni juu ya kina mama kuwanyonyesha wana wao muda wa miaka miwili iliyo timia kwa maslahi ya mtoto mchanga, akitaka hayo mmojapo au wote kati ya wazazi. Itamlazimu baba, kwa kuwa mtoto ni wake, amkimu mama kwa chakula na nguo kwa uwezo wake bila ya israfu wala uchoyo. Kwani

234. Na wale miongoni mwenu wanao kufa na wakaacha wake, hawa wake wangoje peke yao miezi mine na siku kumi. Na wanapo timiza eda yao basi hapana ubaya kwao kwa wanao jifanyia kwa mujibu wa ada. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayo yatenda.²³⁴

235. Wala si vibaya kwenu katika kupeleka posa kwa ishara tu kwa wanawake waliomo edani au mkadhamiria katika nyoyo zenu. Mwenyezi Mungu anajua kwamba nyinyi mtawakumbuka. Lakini msiwaahidi kwa siri, ila mnene maneno mema. Wala msiazimie kufunga ndoa mpaka eda ifike mwisho wake. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo katika nafsi zenu. Basi tahadharini naye. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mpole.²³⁵

236. Hapana ubaya kwenu mkiwapa t'alaka wanawake ambao hamjawagusa au kuwabainishia mahari yao. Lakini wapeni cha kuwaliwaza, mwenye wasaa kadiri awezavyo na mwenye dhiki kadiri awezavyo - maliwaza kwa mujibu wa dasturi kuwa ni haki juu ya watendao mema.²³⁶

237. Na mkiwapa t'alaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea hayo mahari makhsusi, basi wapeni nusu ya mahari mlio agana, isipo kuwa ikiwa wanawake wenyewe wamesamehe, au mume ambaye kifungo cha ndoa ki mikononi mwake awe amesamehe. Na kusameheana ndiko kulio karibu zaidi na uchungu. Wala msisahau fadhila baina yenu. Hakika Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yatenda.²³⁷

haimlazimu mtu kufanya ila kiasi ya uwezo wake, na wala haitakikani kumletea madhara mama kwa kumnyima haki yake ya kumkimu yeye na kumlea mwana. Kadhaalika haitakikani mtoto awe sababu ya kumletea madhara baba yake kwa kumkalifu zaidi kuliko uwezo wake, au kumharimisha haki yake kwa mwanawe. Na akifa baba au akawa fakiri hawezi kazi kiamu kitakuwa juu ya mrithi wa mtoto ikiwa mtoto ana mali yake. Wakitaka wazazi kumwachisha ziwa mtoto kabla ya kutimia miaka miwili wakakubaliana kwa hayo na huku wakiangalia maslaha ya mtoto basi hapana ubaya. Na nyinyi wazazi mkitaka kumpa mama mwingine kumnyonyesha mtoto pia hapana ubaya - na hapo mtamtolea ujira kwa ridhaa na ihsani. Katika myatendayo muangalieni Mwenyezi Mungu, na mjue kuwa Yeye anayajua myatendayo na atakulipeni kwayo. (*Tazama Maelezo 2:233*)

234 Miongoni mwenu enyi wanaume, akitokea aliye kufa akaacha mke asiye na mimba, basi mwanamke yampasa akae eda, yaani asiolewe, muda wa miezi mine ya kuandama na siku kumi mchana na usiku, ili kuhakikisha kiliomo tumboni, kama ana mimba au la. Ukisha muda huu, enyi wazee, hapana ubaya kwenu mkiwaachilia kuleta mtu wa hishima kuja mposa. Haifai nyinyi kuwazuilia hayo, na haijuzu kwao kufanya mambo yanayo kataliwa na Sharia, kwani Mwenyezi Mungu anajua vyema siri zenu na anavijua vitendo vyenu, na atakuhisabuni kwa myatendayo.

235 Katika muda wa eda hapana dhambi kwenu, nyinyi wanaume, mkiwaonyesha dalili kuwa mnadhamiria kutaka kuwao waliomo edani kwa kufiwa na waume zao, lakini hayo yawe ni kudhamiria ndani ya moyo tu. Mwenyezi Mungu hakika anajua kuwa hamwezi kuacha kuwazungumza waliomo edani, kwani ni maumbile baina ya wanaume na wanawake. Kwa hivyo mmepeva ruhusa kuashiria bila ya kubainisha kwa maneno. Basi msiwape ahadi ya kuwao ila iwe ishara isiyo ovu wala ya uchafu. Basi msifunge ndoa mpaka baada ya kwisha eda. Na kuweni yakini kuwa Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yaficha ndani ya nyoyo zenu. Basi iogopeni adhabu yake, wala msitende anayo kukatazeni. Wala msikate tamaa na rehema yake pale mnapo ikhalifu amri yake, kwani Yeye ni Mwenye kughufiria mno, na anakubali toba ya waja wake, na anasamehe makosa, kama alivyo Mpole hafanyi haraka ya kuwaadhibu wale wanao vunja aliyo yakataza.

236 Wala hapana dhambi kwenu enyi waume, wala hapana mahari juu yenu mkiwaacha wake kabla ya kuingia harusi na kabla hamjawatajia kiasi cha mahari. Lakini wapeni zawadi kama kuwapoza kuwapunguzia machungu ya moyo. Na hicho mnacho toa kiwe cha kuridhisha na kupendeza moyo. Tajiri atoe kwa kadiri ya wasaa wake, na fakiri kwa kadiri ya hali yake. Na zawadi hiyo ni katika a'mali za kheri wanazo jilazimisha nazo watu wenye muruwa na watu wa kheri na ihsani.

237 Pindi mkiwapa t'alaka wanawake kabla ya kuingia harusi lakini baada ya kwisha wafikiana mahari,

238. Zilindeni Sala, na khasa Sala ya katikati, na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nanyi ni wenye kuqunuti (kunyenyekoa).²³⁸

239. Ikiwa mnakhofu (Salini) na hali mnakwenda kwa miguu au mmepanda. Na mtakapo kuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama alivyo kufunzeni yale mliyo kuwa hamyajui.²³⁹

240. Na wale miongoni mwenu wanao kufa na wakawacha wake, na wausie kwa ajili ya wake zao kupata matumizi kwa mwaka mmoja bila ya kuwatoa nyumba. Na wanawake wenyewe wakiondoka, basi hapana ubaya kwenu kwa waliyo jifanyia wenyewe kwa mujibu wa Sharia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.²⁴⁰

241. Na wanawake walio achwa wapewe cha kuwaliwaza kwa mujibu wa Sharia. Haya ni waajibu kwa wachamngu.²⁴¹

242. Namna hivi anakubainishieni Mwenyezi Mungu Aya zake ili mpate kufahamu.²⁴²

243. Hukuwaona wale walio toka majumbani kwao kwa maelfu kwa kuogopa mauti? Mwenyezi Mungu akawaambia: Kufeni! Kisha akwahauisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila juu ya watu, lakini wengi wa watu hawashukuru.²⁴³

basi ni haki yao hao wat' alaka wapewe nusu ya mahari, ila wenyewe kwa ridhaa yao wakikataa kuchukua kitu. Na wao pia hawapewi zaidi ya nusu ila waume nafsi zao wakasamehe na wakatoa mahari yote kaamili. Na kila mmoja wapo kusamehe ndio ubora zaidi na ni kumridhisha zaidi Mwenyezi Mungu, na ndio mambo yanavyo elekea kwa wachao Mungu. Basi msiache huu mwendo wa kusameheana. Na kumbukeni kuwa kheri iko katika kufadhiliana na kufanyiana ihsani. Hayo ndiyo yanayo pelekea kupendana baina ya watu. Na Mwenyezi Mungu anazijua vyema dhamiri zenu na atakulipeni kwa fadhila mzitendazo.

238 Fanyeni hima katika kusimamisha Sala zote na kuzidumisha. Na fanyeni hima kuwa Sala yenu iwe ni Sala bora kwa kuzitimiza nguzo zake na kumsafia niya Mwenyezi Mungu kwa ukamilifu katika Sala. Na timizeni ut'iifu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na mkumbukeni kwa usafi wa moyo na kunyenyekea Utukufu wake.

239 Ukikufikieni wakati wa Sala nanyi mko katika khofu basi msiache kusali, bali salini kama muwezavyo, ikiwa huku mnakwenda kwa miguu au mmepanda kipando. Ikiondoka khofu salini kwa kutimiza nguzo zote kama mlivyo jifunza, mkimkumbuka Mwenyezi Mungu katika Sala na mkimshukuru kwa alivyo kufunzeni, na kwa kukujaalieni kuwa katika amani.

240 Wanao kufa miongoni mwenu wakaacha wake zao, Mwenyezi Mungu ameusia hao wanawake wafiwa wabaki nyumbani mwa waume zao muda wa mwaka mzima kwa maliwaza na kuwaondolea ukiwa. Wala hana haki yeyote kuwatoa. Wakitoka kwa khiari yao kabla ya mwaka kwisha basi hamna dhambi nyinyi wenye madaraka mkiwaachilia wajitendee wenyewe wapendalo kwa lisio vunja Sharia tukufu. Na mt'iini Mwenyezi Mungu katika hukumu zake, na tendeni Sharia alizo kutungieni kwani Yeye ni Muweza wa kumuadhibu anaye kwenda kinyume na amri yake, na Yeye ni Mwenye hikima iliyo pita ukomo. Hakuamrinishi ila lenye maslaaha yenu ijapo kuwa hikima yake imepindukia ujuzi wenu.

241 Na wanawake walio pewa t' alaka baada ya kuingia harusi wana haki wapewe mali ya kuwaliwaza. Wapewe kwa wema, kwa kadiri ya utajiri na umasikini wa mume. Kumcha Mwenyezi Mungu kunawajibisha hayo, na pia watu wa Imani wanalazimika na hayo.

242 Mwenyezi Mungu anakubainishieni hukumu zake, na neema zake, na Aya zake, kwa mfano wa bayana hizi na Sharia hizi zilizo wazi zenye kuleta maslaaha, ili mpate kuzingatia na mpate kutenda yalivyo kheri.

243 Zingatia, ewe Nabii, hichi kisa cha ajabu, na ukijue! Hao watu walitoka wakaacha majumba yao ati wanakimbia Jihadi kwa kuogopa kufa, na hali wao ni maelfu kwa maelfu. Mwenyezi Mungu akawahukumia kifo na udhalili kutokana na maadui zao. Walipo bakia walio bakia wakasimama kupigana Jihadi, Mwenyezi Mungu aliwapa uhai kwa kuwapa nguvu. Hakika uhai huu wenye nguvu ulio kuwa baada ya madhila umekuja kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu, na unastahiki shukrani. Lakini wengi wa watu hawashukuru.

244. Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Msikizi na Mjuzi.²⁴⁴

245. Ni nani atakaye mkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema ili amzidishie mzidisho mwingi, na Mwenyezi Mungu hukunja na hukunja. Na Kwake Yeye mtarejea.²⁴⁵

246. Hukuwaona watukufu katika Wana wa Israili baada ya Musa, walipo mwambia Nabii wao: Tuwekee mfalme ili tupigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Akasema: Je, haelekei ikiwa mtaandikiwa vita kuwa msipigane? Wakasema: Itakuwaje tusipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali tumetolewa majumbani kwetu na watoto wetu? Lakini walipo andikiwa kupigana waligeuka, isipo kuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anawajua madhaalimu.²⁴⁶

247. Na Nabii wao akawaambia: Mwenyezi Mungu amekuteulieni Taluti (Sauli) kuwa ni mfalme. Wakasema: vipi atakuwa na ufalme juu yetu, na hali sisi tuna haki zaidi kupata ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali? Akasema: Mwenyezi Mungu amemteua yeye juu yenu na amemzidishia ukunjufu wa ilimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mjuzi.²⁴⁷

248. Na Nabii wao akawaambia: Alama ya ufalme wake ni kukuleteeni lile sanduku ambalo mna ndani yake kituliza nyoyo zenu, kitokacho kwa Mola wenu Mlezi, na mna mabaki ya waliyo yaacha kina Musa na kina Harun, wanalichukua Malaika. Bila

244 Mlivyo jua kuwa hamwezi kuyaepuka mauti kwa kuyakimbia, basi piganeni Jihadi, na zitumieni nafsi zenu kwa kulitukuza Neno la Mwenyezi Mungu, na kuweni na yakini kuwa Mwenyezi Mungu anayasikia wanayo yasema woga na wanaafiki wanao kimbia, na wayasemayo Mujaahidina wanao pigana, na anayajua anayo dhamiria kila mtu katika nafsi yake. Na kwa lilio kheri atamlipa kheri, na kwa shari atamlipa shari.

245 Na Jihadi kwa Njia ya Mwenyezi inhaitaji mali, basi toeni mali yenu. Mtu gani huyo ambaye hatoi mali yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa radhi ya nafsi yake, na hali Mwenyezi Mungu ameahidi kuwa atamrejeshea mara nyingi sana zaidi? Na riziki zote zimo katika mkono wa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye humkunja amtakaye na akamkunjulia amtakaye kwa yaliyo na maslaha yenu. Marejeo ni kwake Yeye, naye atakulipeni kwa mujibu mlivyo toa. Na ilivyo kuwa riziki zote ni kwa fadhila ya Mwenyezi na Yeye ndiye mwenye kutoa na mwenye kunyima basi ameitwa yule mwenye kutoa kuwa ni kama mkopeshaji ili kuhimiza na kupendekeza kutoa, na kutilia mkazo kuwa malipo ni mara nyingi sana duniani na Akhera.

246 Zingatia khabari hii ya ajabu ya baadhi ya Wana wa Israili baada ya zama za Musa. Walimtaka Nabii wao wa wakati ule awawekee mtawala ataye weza kuwakusanya baada ya mfarakano walio kuwa nao, awaongoze chini ya bendera ya kutukuza Neno la Mwenyezi Mungu na kurejeza utukufu wao. Yule Nabii akawauliza kuhakikisha kama wana ukweli katika jambo hilo: “Je haiwezi kuwa nyinyi mtaingia woga mkatae kupigana pindi mkifaridhiwa mpigane?” Wakakataa hayo wakisema: “Itakuwaje tusipigane kurejeza haki zetu, na hali sisi tumefukuzwa makwetu na adui?” Mwenyezi Mungu alipo waitikia yale wayatakayo na akaandikia vita wakakataa ila kikundi cha wachache tu miongoni mwao. Na kule kukataa kwao ni dhulma kujidhulumu nafsi zao, na Nabii wao na Dini yao. Na Mwenyezi Mungu anayajua hayo kwao, na atawalipa malipo ya madhaalimu.

247 Nabii wao akawaambia: “Hakika Mwenyezi Mungu amekuitikieni, basi amemkhiari Taluti awe ndiye mtawala wenu.” Wakuu wao wakapinga huo uteuzi wa Mwenyezi Mungu, wakisema: “Kwa nini awe yeye ni wa kututawala na hali sisi ni bora kuliko yeye. Yeye si mtu wa ukoo bora wala hana mali.” Nabii wao akawarudi kwa kusema: “Mwenyezi Mungu amemkhiari yeye kuwa ni mtawala wenu kwa sababu ana sifa nyingi za uwongozi, kama mazoezi makubwa katika mambo ya vita, na siyasa ya kutawala, pamoja na nguvu za mwili. Na utawala uko katika mkono wa Mwenyezi Mungu humpa amtakaye katika waja wake, wala yeye hatagemei urithi wala mali.” Na fadhila za Mwenyezi Mungu na ujuzi wake umeenea. Yeye huchagua lilio na maslaha yenu.

shaka katika hayo zimo dalili kwenu ikiwa nyinyi mnaamini.²⁴⁸

249. Basi Taluti alipo ondoka na majeshi alisema: Mwenyezi Mungu atakujaribuni kwa mto. Atakaye kunywa humo si pamoja nami, na asiye kunywa atakuwa pamoja nami: ila atakaye teka kiasi ya kitanga cha mkono wake. Lakini walikunywa humo isipo kuwa wachache tu miongoni mwao. Alipo vuka mto yeye na wale walio amini pamoja naye, walisema: Leo hatumwezi Jaluti (Goliati) na majeshi yake. Wakasema wale wenye yakini ya kukutana na Mwenyezi Mungu: Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wenye kusubiri.²⁴⁹

250. Na walipo toka kupambana na Jaluti na majeshi yake walisema: Mola wetu Mlezi! Tumiminie subira, na isimamishe imara miguu yetu, na utusaidie tuwashinde watu Makafiri--²⁵⁰

251. --Kwa idhini ya Mwenyezi Mungu waliwatimua, na Daudi akamuwa Jaluti, na Mwenyezi Mungu akampa Daudi ufalme na hikima, na akamfundisha aliyo yapenda. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawapambanishi watu kwa watu basi dunia ingeli haribika. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila juu ya walimwengu wote.²⁵¹

252. Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu tunakusomea kwa haki. Na hakika wewe ni miongoni mwa Mitume.²⁵²

253. MITUME hao tumewatukuza baadhi yao juu ya wengineo. Katika wao wapo ambao Mwenyezi Mungu alisema nao, na wengine akawapandisha vyeo. Na tukampa Isa mwana wa Mariyam hoja zilizo wazi, na tukamtia nguvu kwa Roho Takatifu. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu alipenda wasingeli pigana walio kuwa baada yao baada

248 Na Nabii wao aliwaambia: "Hakika dalili ya ukweli wangu kuwa Mwenyezi Mungu amemteua Taluti awe ni mtawala wenu ni kuwa atakurejesheeni sanduku la Taurati mlio nyang'anywa, linalo bebwa na Malaika. Na ndani yake yamo baadhi ya mabaki ya watu wa Musa na watu wa Harun walio kuja baada yao. Na likiletwa sanduku hilo nyoyo zenu zitataua. Katika hayo hakika pana dalili ambazo zitakupelekeeni kumfuata na kumridhia, ikiwa kama kweli nyinyi mnataka Haki na mnaamini."

249 Taluti alipo toka nao aliwaambia: "Mwenyezi Mungu anakujaribuni kwa mto ambao mtaukuta njiani mwenu. Msinywe katika mto huo ila tama moja tu. Mwenye kunywa zaidi ya hivyo basi hayumo katika jeshi letu, wala jamii yetu. Kwani amekuwa ameacha kum'tii Mwenyezi Mungu. Wala asinifuate ila yule ambaye hakunywa ila tama moja tu." Hawakuweza kuvumilia jaribio hili, wakanywa maji mengi, ila wachache tu kati yao. Basi akafuatana na hichi kikundi kidogo akavuka nao mto. Walipoona wingi wa maadui wao walisema: "Hatutoweza hii leo kupigana na Jaluti na askari wake kwa wingi wao na uchache wetu." Baadhi yao wenye nyoyo madhbuti kwa kutaraji kwao malipo ya Mwenyezi Mungu watapo kutana naye, walisema: "Msiogope kitu! Mara nyingi wachache wenye kuamini huwashinda wengi walio makafiri. Subirini, kwani ushindi watapata wenye kusubiri."

250 Waumini walipo songa kupigana na Jaluti na jeshi lake walimwelekea Mwenyezi Mungu wakamnyenyekea na kumwomba awajaze subira, awatie nguvu azma zao, naawaweke imara katika uwanja wa vita, na awape ushindi juu ya maadui zao makafiri.

251 Basi wale Waumini waliwashinda maadui zao kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na Daudi, mmoja wa askari wa Taluti, akamwuuwa Jaluti amiri-jeshi wa makafiri. Na Mwenyezi Mungu akampa Daudi utawala baada ya Taluti. Akampa na unabii na ilimu yenye manufaa, na akamfunza kwa ayapendayo Mwenyezi Mungu. Na huo ndio mwendo wake Mwenyezi Mungu - kuwanusuru wale wanao tenda mema duniani wala hawafanyi ufisadi. Lau kuwa Mwenyezi Mungu hawasalitishi askari wake kupambana na mafisadi kwa ajili ya kuondoa ufisadi wao, na akawasalitisha waovu wenyewe kwa wenyewe, ulimwengu usingeli endelea. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye hisani na fadhila daima milele juu ya waja wake.

252 Kisa hichi ni katika mafunzo ya kuzingatia tunakusimulia kwa kweli, ili kiwe ni ruwaza kwako na dalili ya ukweli wa Utume wako, na ili ujue kuwa Sisi hakika tutakunusuru kama tulivyo wanusuru Mitume walio kuwa kabla yako.

ya kuwajia hoja zilizo wazi. Lakini walikhitalifiana. Basi wapo kati yao walio amini, na wengine kati yao walio kufuru. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu alipenda wasingeli pigana. Lakini Mwenyezi Mungu hutenda atakavyo.²⁵³

254. Enyi mlio amini! Toeni katika tulivyo kupeni kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwapo biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndio madhaalimu.²⁵⁴

255. Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala. Ni vyake pekee vyote viliomo mbinguni na duniani. Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; wala wao hawajui chochote katika vilio katika ujuzi wake, ila kwa atakalo mwenyewe. Enzi yake imetanda mbinguni na duniani; na wala haemewi na kuvilinda hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu.²⁵⁵

256. Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anaye mkataa Shet'ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.²⁵⁶

257. Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walio amini. Huwatoa gizani na kuwaingiza mwangazani. Lakini walio kufuru, walinzi wao ni Mashet'ani. Huwatoa kwenye

253 Hao ni Mitume ambao baadhi yao tumewataja, wengine tumewatukuza kuliko wenginewe. Wamo kati yao walio semezwa na Mwenyezi Mungu ana kwa ana, kama Musa. Na wengine kati yao Mwenyezi Mungu amewanyanyua kushinda vyeo vya wote, kama Muhammad ambaye akamkhusisha kumpa Ujumbe kwa ulimwengu wote, na kukamilisha Sharia, na kuwa ni Mtume wa mwisho. Na miongoni mwao ni Isa bin Maryam, ambaye Mwenyezi Mungu alimtia nguvu kwa kumpa miujiza kama kufufua wafu, na kuponyesha upofu na ukoma, na akamletea Jibril, Roho Mtakatifu, ili kumtia nguvu. Na Mitume hawa wameleta Uwongofu, na Dini ya Haki, na Ushahidi ulio wazi wenye kuongoa. Kwa haya imewajibikia watu wote wawaamini, wala wasikhitalifiane, wala wasipigane. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu alipenda wasipigane hao watu baada ya kuletewa Mitume na ishara zilizo wazi zenye kuonyesha Haki, pasingetokea kupigana wala kukhitalifiana. Lakini Mwenyezi Mungu hakutaka hayo. Kwa hivyo wakakhitalifiana. Basi kati yao wakawapo walio amini, na wengine walio kufuru. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu alipenda wasingeli uwana wala wasingeli khitalifiana. Bali wangeli kuwa wote katika Haki. Lakini Mwenyezi Mungu hutenda apendalo.

254 Enyi mlio muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho! Toeni baadhi ya tuliyo kuruzukuni kwa ajili ya mambo ya kheri. Fanyeni haraka kwa hayo kabla haijafika Siku ya Kiyama ambayo itayo kuwa yote ni ya kheri, wala hazipatikani sababu za kuzozana. Siku hiyo hamwezi kuyadiriki yaliyo kwisha kupiteni duniani, na hapo haitakufaeni biashara, wala urafiki, wala uombezi wa mtu yeyote bila ya idhini ya Mwenyezi Mungu. Na siku hiyo dhulma za makafiri zitadhihiri kwa kuwa hawakuitikia Wito wa Haki.

255 Mwenyezi Mungu ndiye anaye stahiki kuabudiwa pekee. Yeye ndiye Mwenye kubaki, Mwenye kuyasimamia mambo ya viumbe daima. Haghafiliki kabisa, wala hanyong'onyei, wala halali (1) wala yanayo fanana na hayo, kwani Yeye hasifikwi na upungufu wa chochote. Yeye pekee ndiye Mwenye kumiliki mbingu na ardhi, wala hana mshirika yeyote katika hayo. Kwa hivyo hapana kiumbe anaye weza kumwombea mwenginewe ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Yeye *Subhanahu wa Taa'la* anajua kila kitu. Anayajua yaliyo kuwa na yatayo kuwa. Hapana mtu anaye weza kujua kitu katika ilimu ya Mwenyezi Mungu ila atakavyo Yeye ajue na aridhie. Utawala wake umeenea mbinguni na ardhini. Hayamhangaishi Yeye kuyadabiri hayo, kwani Yeye ametukuka, hana upungufu wala kushindwa na jambo, Muadhamu katika utukufu wake na utawala wake. (*Tazama Maelezo 2:255*)

256 Hapana ruhusa kumlazimisha yeyote kuingia katika Dini. Kwa Aya na Ishara zilizo zagaa Njia ya Haki imewekwa wazi kutokana na njia ya upotovu. Basi aliye ongoka akafuata Imani na akakataa kufuata chochote kisicho ingia akilini, na kinacho mpelekea kuacha Haki, basi huyo ameshika njia madhubuti kabisa ya kumkinga asiingie katika upotovu, kama yule mwenye kukamata kishikio imara kilicho fungika baraabara kitacho mlinda asitumbukie shimoni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyasikia mnayo yasema, ni Mwenye kuyajua mnayo yatenda, na ni Mwenye kukulipeni kwa vitendo vyenu.

mwangaza na kuwaingiza gizani. Hao ndio watu wa Motoni, na humo watadumu.²⁵⁷

258. Hukumwona yule aliye hojiana na Ibrahim juu ya Mola wake Mlezi kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa ufalme? Ibrahim alipo sema: Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na kufisha. Yeye akasema: Mimi pia nahuisha na kufisha. Ibrahim akasema: Mwenyezi Mungu hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi. Akafedheheka yule aliye kufuru; na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.²⁵⁸

259. Au kama yule aliye pita karibu na mji ulio kwisha kuwa magofu tu, akasema: Ataufufuaje Mwenyezi Mungu mji huu baada ya kufa kwake? Basi Mwenyezi Mungu alimfisha yeye muda wa miaka mia. Kisha akamfufua. Akamuuliza: Je umekaa muda gani? Akajibu: Labda nimekaa siku moja au sehemu ya siku. Akamwambia: Bali umekaa miaka mia wewe. Hebu angalia chakula chako na vinywaji vyako, havikuharibika. Na muangalie punda wako. Na ili tukufanye uwe ni Ishara kwa watu iangalie hii mifupa yake jinsi tunavyo inyanuya kisha tunaivisha nyama. Basi yalipo mbainikia alinena: Najua kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.²⁵⁹

260. Na alipo sema Ibrahim: Mola wangu Mlezi! Nionyeshe vipi unavyo fufua wafu. Mwenyezi Mungu akasema: Kwani huamini? Akasema: Hasha! Lakini ili moyo wangu utue. Akamwambia: Twaa ndege wane na uwazeshe kwako, kisha uweke juu ya kila kilima sehemu, kisha wete, watakuja mbio. Na ujue kwamba hakika Mwenyezi

257 Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuyaangalia mambo ya Waumini, na ndiye Mwenye kuwasaidia na kuwanusuru. Huwatoa kwenye kiza cha shaka na kudanganyikiwa kuendea kwenye nuru ya Haki na utulivu. Na Makafiri wenye kumkanya Mwenyezi Mungu wanashughulikiwa na Mashetani na wanao lingania shari na upotovu. Wao hao huwatoa kwenye nuru ya Imani walio umbiwa nayo na iliyo zagaa kwa dalili nyingi na ishara, na kuwatia kwenye kiza cha ukafiri na uufisadi. Na hawa makafiri ndio watu wa Motoni, na humo watadumu milele.

258 Humwoni yule aliye pofuka asizone dalili za Imani akajadiliana na Ibrahim, rafiki wa Mwenyezi Mungu, katika ungu wa Mola wake Mlezi na Umoja wake, na vipi alivyo danganyika na ufalme wake alio pewa na Mola wake Mlezi hata akatoka kwenye nuru ya maumbile akaingia katika kiza cha ukafiri? Alipo sema Ibrahim: Mwenyezi Mungu huhuisha na hufisha, kwa kuitia roho katika kiwiliwili na kuitoa, yule mfalme kafiri akasema: Nami nahuisha na ninafisha kwa kusamehe na kuuwa. Basi Ibrahim akamwambia ili kuyakata majadiliano: Mwenyezi Mungu analichomozesha jua mashariki, basi wewe lileta litoke magharibi kama wewe ni mungu kama unavyo dai. Akahizika, na majadiliano yakakatika kwa nguvu za hoja zilizo kashifu udhaifu wake na kughurika kwake. Na Mwenyezi Mungu hawawezeshi wakaidi na wenye inadi kufuata Haki.

259 Kisha zingatia kisa hichi cha ajabu, cha mtu aliye pita kwenye mji uliyo kwisha teketea, sakafu za majumba yake zimeporomoka na zimebomoa viwambaza vyake, na watu wake wameangamia. Akasema huyo mtu: Vipii Mwenyezi Mungu atawahuisha tena watu wa mji huu baada ya kuwa wamekwisha kufa? Mwenyezi Mungu akamfisha yeye na akamweka, naye ni maiti, muda wa miaka mia. Kisha akamfufua, ili amwonyeshe wepesi wa ufufuaji na imtoke shaka. Kisha akamwuliza: Umekaa muda gani nawe maiti? Akajibu, naye hajui urefu wa muda wake: Siku moja, au sehemu ya siku. Akaambiwa: Bali umekaa, nawe ni mfu, muda wa miaka mia. Kisha akaonyesha jambo jengine kuwa ni dalili ya uweza wa Mwenyezi Mungu. Akamwambia: Angalia chakula chako hakikuchacha, na vinywaji vyako havikutaghayari. Aidha muangalie punda wako. Na hayo tumeyafanya ikudhihirikie uliyo dhani hayawi, ya kufufuliwa vilio kufa, na tukufanye wewe uwe ni Ishara ya kuwaonyesha watu ukweli wa kufufuliwa. Kisha Mwenyezi Mungu akaamrisha atazame maajabu ya kuumba kwake vilivyo na uhai, na vipi anairekibisha mifupa, na kuivisha nyama, kisha akaitia roho vikawa vinataharaki. Basi ulipo mfungukia yule mtu uweza wa Mwenyezi Mungu, na wepesi wa kufufua, alisema: Najua kuwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, na Mwenye hikima.²⁶⁰

261. Mfano wa wanao tumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyo chipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua.²⁶¹

262. Wanao toa mali zao kwa Njia ya Mwenyezi Mungu, kisha hawafuatishii masimbulizi wala udhia kwa walicho toa, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.²⁶²

263. Kauli njema na usamehevu ni bora kuliko sadaka inayo fuatiliwa na maudhi. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitoshia na Mpole.²⁶³

264. Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi, kama anaye toa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Basi mfano wake ni kama mfano wa jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa, ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza wowote kwa walivyo chuma. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri.²⁶⁴

265. Na mfano wa wale wanao toa mali zao kwa kuitafuta radhi ya Mwenyezi Mungu na kuzipa nguvu roho zao ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu, ikaifikia mvua kubwa na ikaleta mazao yake mardufu; na hata kama haifikikiwi na mvua kubwa basi manyunyu hutosha. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yatenda.²⁶⁵

260 Kitaje pia kisa cha Ibrahim alipo sema: Mola wangu Mlezi nionyeshe vipi unahuisa maiti. Mola wake Mlezi akamuuliza Ibrahim, juu ya imani yake kuamini kufufuliwa wafu, ili ajibu Ibrahim kuondoa shaka kabisa katika imani yake. Mwenyezi Mungu akamwambia: Kwani huamini kufufuliwa wafu? Ibrahim akajibu: Mimi naamini, lakini nimetaka ili moyo uzidi kutua. Akasema Mwenyezi Mungu: Basi wachukue ndege wane uwe nao ili uwajue vilivyo. Kisha uwagawe baada ya kuwachinja, na juu ya kila kilima katika vilima vilio jirani weka sehemu yao. Kisha uwete, watakujia mbio, nao ni wahai kama walivyo kuwa. Na jua kuwa Mwenyezi Mungu hashindwi na lolote. Naye ni Mwenye hikima iliyo pita hadi katika kila kitu. (*Tazama Maelezo 2:260*)

261 Hakika hali ya wale wanao toa mali yao kwa ajili ya kumt'ii Mwenyezi Mungu na kufanya kheri, na wanapata kwa hivyo thawabu za kuzidia mara nyingi, ni kama hali ya mwenye kuatika punje moja katika ardhi yenye rutuba ikamea mmea wenye mashuke saba, katika kila shuke mna punje mia. Hii ni ya wingi wa Mwenyezi Mungu anavyo walipa wanao toa katika dunia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakae. Yeye ni Mwenye wasaa wa fadhila, Mwenye kuwajua wanao stahiki na wasio stahiki.

262 Hakika wanao toa mali kwa ajili ya wema unao kubaliwa na sharia bila ya kusimbulia au kutafakhari au kumchelewesha yule anaye fanyiwa hisani, hao wana malipo bora walio ahidiwa kwa Mola wao Mlezi, wala haiwapati khofu kwa lolote wala huzuni.

263 Kauli ya kupoza nyoyo na ya kumsitiri hali fakiri usimwambie mwenginewe ni bora kuliko kumpa na baadae ukafuatizia maudhi kwa maneno au vitendo. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* si mwenye kuhitaji watu watoe na huku wanawaudhi mafakiri. Na Yeye anawawezesha mafakiri kupata riziki njema. Wala hafanyi haraka kumuadhibu asiye toa kwa matarajio huenda akaongoka akatoa.

264 Enyi Waumini! Msipoteze thawabu za sadaka zenu kwa kudhihirisha kuwa mnawafadhili wenye haja na kuwaudhi. Hivyo mnakuwa kama wale wanao toa mali zao kwa ajili ya kutafuta umaarufu na kupenda wasifiwe na watu., nao hata hawamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Hali ya mwenye kuonyesha kutoa kwake ni hali ya jiwe manga lenye udongo. Likateremkiwa na mvua kubwa, udongo wote ukaondoka. Basi kama mvua kubwa inavyo chukua udongo wenye mbolea likabaki jiwe tupu, basi kadhaalika masimbulizi, na maudhi, na kuonyesha watu huharibu thawabu za sadaka. Hayo hayamnufaishi mtu, na hizo ni sifa za makafiri. Epukaneni nazo! Kwani Mwenyezi Mungu hawawafikishi makafiri kupata kheri na uwongozi mwema.

265 Hali ya wanao toa mali zao kwa kutaka kumridhi Mwenyezi Mungu na kuzithibitisha nafsi zao juu ya Imani, ni kama hali ya bustani, au kitalu, kwenye ardhi yenye rutuba iliyo nyanyuka inayo faidika kwa maji mengi au kidogo. Ikija mvua kubwa huzaa mazao yake mardufu; na ikitopata mvua kubwa basi

266. Je! Yupo mmoja wenu anaye penda kuwa na kitalu cha mitende na mizabibu ipitayo mito kati yake, naye humo hupata mazao ya kila namna, na uzee ukamfikia naye hali ana watoto wanyonge, kikapigwa na kimbunga chenye moto, kikaungua? Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo kubainishieni Ishara ili mpate kufikiri.²⁶⁶

267. Enyi mlio amini! Toeni katika vile vizuri mlivyo vichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msinge vipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitoshia na Msifiwa.²⁶⁷

268. Shet'ani anakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Mwenyezi Mungu anakuahidini msamaha na fadhila zitokazo kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.²⁶⁸

269. Yeye humpa hikima amtakaye; na aliye pewa hikima bila ya shaka amepewa kheri nyingi. Na hawakumbuki ila wenye akili.²⁶⁹

270. Na chochote mnacho toa au nadhiri mnazo weka basi hakika Mwenyezi Mungu anajua. Na walio dhulumu hawana wa kuwanusuru.²⁷⁰

271. Mkizidhihirisha sadaka ni vizuri; na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni kheri kwenu, na yatakuondoleeni baadhi ya maovu yenu. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.²⁷¹

hata manyunyu kidogo hutoshia kwa vile ardhi ni nzuri yenye kutoa mazao katika hali zote mbili. Basi Waumini wenye nyoyo safi hazipoteti a'mali zao. Na vitendo vyenu havifichiki kwa Mwenyezi Mungu. (Tazama Maelezo 2:265)

266 Hapana yeyote katika nyinyi anaye penda kuwa na kitalu cha mitende na mizabibu na mito inapita kati yake na kimezaa kila namna ya matunda ayatakayo, naye hali amekwisha kuwa mkongwe na akawa na watoto wadogo wanyonge hawawezi kazi wala yeye hajiwezi kwa ukongwe wake, kikaja kitalu chake kikakauka kwa upepo mkali wenye moto, na miti ikaungua, wakati ambao yeye mwenyewe na watoto ndio wamo katika shida ya kuhitaji. Basi hali kadhaalika shani ya mwenye kutoa sadaka na akafuatishia masambulizi na maudhi na riya, kujionyesha kwa watu, ambayo hayo yakapoteza thawabu zote za sadaka zake, na wala hawezi tena kutoa sadaka kwa kujitengezea nafsi yake. Kwa bayana kama hizi ndio Mwenyezi Mungu anakuonyesheni Ishara ili mpate kutafakiri na kujifunza. (Tazama Maelezo 2:266)

267 Enyi Waumini! Toeni bora ya mnacho kipata kwa juhudi yenu, na ambacho mlicho wezesha kukitoka katika ardhi, ikiwa kwa makulima, au maadini au chenginecho. Wala msikusudie kutoa kile kilicho duni na kibaya katika mali, na ilhali nyinyi msinge kubali kuchukua hivyo ila ingeli kuwa mmegubikwa macho au hamuoni huo ubaya. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu si mwenye haja ya sadaka zenu, na Yeye ni mwenye kustahiki kila sifa njema na shukrani kwa alivyo kuongozeni kuendea kheri na wema.

268 Shetani anakutieni khofu kuwa mtafakirika kwa kutoa, na kazi yake kutia ila kila kitendo chema, ili msitoe kwa ajili ya mambo ya kheri na mghurike na maasi. Na Mwenyezi Mungu aliye Mkunjufu wa kusamehe, ni Muweza wa kukutoshelezeni. Hapana lolote katika mambo yenu linalo fichikana kwake.

269 Yeye humpa sifa ya Hikima, kusema na kutenda lilio la haki, ampendaye kati ya waja wake. Na mwenye kupewa hayo basi kapewa kheri nyingi, kwani kwayo ndio hutengenea mambo ya duniani na Akhera. Na wala hawanafiki kwa waadhi na mazingatio ya amali za Qur'ani ila wale wenye akili sawa inayo tambua ukweli bila ya kupindukia mipaka kwa pumbao la ufisadi.

270 Na kila mnacho kitoa, ikiwa kwa kheri au shari, au mnacho lazimika kutoa kwa ut'iifu, basi Mwenyezi Mungu anakijua na atakulipeni. Na wale wenye kudhulumu, wanao toa kwa ajili ya kujionyesha kwa watu au wale wanapo toa wanawaudhi masikini za Mungu, au wanao toa kwa ajili ya maasi, hawatakuwa na watu wa kuwanusuru na adhabu ya Mwenyezi Mungu huko Akhera.

271 Na ikiwa mtazidhihirisha sadaka zenu, bila ya makusudio ya kutaka kujionyesha kwa watu, ni vizuri kwenu, inapendeza, na kwa Mola wenu Mlezi inasifika. Na pindi mkiwapa mafakiri kwa siri ili msiwatie haya, na kwa kuogopa riya (kujionyesha), basi nayo ni kheri kwenu. Na Mwenyezi Mungu atakusameheni dhambi zenu kwa sababu ya usafi wa niya zenu katika kutoa sadaka zenu. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yaficha na mnayo yadhahirisha, na anazijua niya zenu mnapo dhahirisha na

272. Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye. Na kheri yoyote mnayo toa ni kwa nafsi zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta wajihi wa Mwenyezi Mungu. Na kheri yoyote mtakayo toa mtalipwa kwa ukamilifu, wala hamtadhulumiwa.²⁷²

273. Nawapewe mafakiri walio zuilika katika njia za Mwenyezi Mungu, wasio weza kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Asiye wajua hali zao huwadhanika kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao. Utawatambua kwa alama zao; hawang'ang'analii watu kwa kuwaomba. Na kheri yoyote mnayo toa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu anajua.²⁷³

274. Wale wanao toa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.²⁷⁴

275. Wale walao riba hawasimami ila kama anavyo simama aliye zugwa na Shet'ani kwa kungusa. Hayo ni kwa kuwa wamesema: Biashara ni kama riba. Lakini Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na ameharimisha riba. Basi aliye fikiwa na mawaidha kutoka kwa Mola wake Mlezi, kisha akajizuia, basi yake ni yaliyo kwisha pita, na mambo yake yako kwa Mwenyezi Mungu. Na wenye kurudia basi hao ndio watu wa Motoni, humo watadumu.²⁷⁵

276. Mwenyezi Mungu huiondolea baraka riba, na huzibariki sadaka. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila mwenye kukanya na afanyae dhambi.²⁷⁶

277. Hakika wale walio amini na wakatenda mema na wakashika Sala na wakatoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao,

mnapo ficha.

272 . Si juu yako wewe, ewe Muhammad, kuwaongoa hao walio potea au kuwalazimisha watende kheri. Lilio juu yako ni kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye. Na msaada wowote mnao toa kumpa mtu, faida yake inarejea kwenu wenyewe. Mwenyezi Mungu atakulipeni kwayo. Haya ni hivyo ikiwa mnapo toa hamkusudii ila kumridhi Mwenyezi Mungu. Na kheri yoyote mnayo itoa kwa njia hii itarejea kwenu, na mtazipata thawabu zake kwa ukamilifu bila ya kudhulumiwa chochote.

273 Na kutoa huko ni kwa kuwapa mafakiri ambao kwa sababu ya kuwania jihadi hawawezi kujichumia wenyewe, au ambao kwa sababu ya kuumia katika jihadi wameemewa na kuweza kuhangaika katika nchi kutafuta riziki. Na juu ya hivyo wanajizuia na kuomba omba. Asiye wajua huwadhanika kuwa ni matajiri, lakini wewe utajua hali yao kwa alama zake. Na kila mtacho kitoa kwa wema, basi Mwenyezi Mungu anakijua, naye atakulipeni malipo ya kutosha.

274 Wale ambao dasturi yao ni kutoa kwa ukarimu wa nafsi zao usiku na mchana, mbele za watu na katika siri, watapata malipo yao kutokana na Mola wao Mlezi. Hawatofikiwa na khofu yoyote baadae, wala hawatakuwa na huzuni kwa kukosa chochote.

275 Wale kazi yao ni kula riba hawawi katika juhudi yao na mambo yao yote ila ni kuhangaika tu na kushughulika ovyo, kama aliye haribiwa akili yake na Shetani, akawa anateseka na wazimu ulio msibu. Kwani wao hudai kuwa biashara ni kama riba, kwa kuwa zote mbili hizi ni kutoa na kuchuma. Basi yapasa, kwa madai yao, njia zote hizo ziwe ni halali. Mwenyezi Mungu amewarudi hayo madai yao, kwa kubainishia kuwa kuhahalalisha na kuharimisha si katika madaraka yao, na huko kufananisha kwao si kweli kabisa. Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara, na ameharimisha riba. Basi mwenye kufikiliwa na amri ya Mola wake Mlezi ya kuharimishwa riba na akaifuata, basi imthibitike ile riba aliyo ichukua kabla ya kuja amri ya kuharimishwa. Na hukumu yake iko mikononi mwa Mwenyezi Mungu akitaka kumsamehe. Lakini wenye kurejea kula riba wakaifanya ni halali, baada ya kwisha harimishwa, hao watalazimika kudumu Motoni. (*Tazama Maelezo 2:275*)

276 Mwenyezi Mungu huondoa ile ziada iliyo twaliwa kuwa ni riba juu ya mali yaliyo kopeshwa, na huitilia baraka mali iliyo tolewa sadaka, na huilipia thawabu mara nyingi kuliko kile kilicho tolewa. Na Mwenyezi Mungu hawapendi watu wanao endelea kuhahalalisha haramu kama riba, wala wale wanao endelea kuchukua riba.

wala hawatahuzunika.²⁷⁷

278. Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na acheni riba zilizo bakia, ikiwa nyinyi ni Waumini.²⁷⁸

279. Basi mkitofanya jitangazieni vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mkitubu, basi haki yenu ni rasilmali zenu. Msidhulumu wala msidhulumiwe.²⁷⁹

280. Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike. Na mkiifanya deni kuwa ni sadaka, basi ni bora kwenu, ikiwa mnajua.²⁸⁰

281. Na iogopeni Siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila nafsi italipwa ilicho chuma. Nao hawatadhulumiwa.²⁸¹

282. Enyi mlio amini! Mnapo kopeshana deni kwa muda ulio wekwa, basi andikeni. Na mwandishi aandike baina yenu kwa uadilifu, wala mwandishi asikatae kuandika. Aandike kama alivyo mfunza Mwenyezi Mungu. Na mwenye deni juu yake aandikishe; naye amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi. Wala asipunguze chochote ndani yake. Na akiwa mwenye kudaiwa ni mtu aliye pumbaa au mnyonge au hawezi kuandikisha mwenyewe, basi aandikishe mlinzi wake kwa uadilifu. Na mshuhudishe mashahidi wawili katika wanaume wenu. Ikiwa hapana wanaume wawili, basi mwanamume mmoja na wanawake wawili katika mnao waridhia kuwa mashahidi. Ili ikiwa mmoja wao akipotea, mmoja wao amkumbushe mwengine. Na mashahidi wasikatae waitwapo. Wala msipuuze kuliandika deni likiwa dogo au kubwa mpaka muda wake. Hayo ndiyo haki zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu, na ndiyo sawa zaidi kwa ushahidi, na vyema zaidi ili msiwe na shaka. Ila ikiwa ni biashara ya mkono-kwa-mkono baina yenu, basi hapo si vibaya kwenu msipo iandika. Lakini mnapo uziana wekeni mashahidi. Wala asitiwe matatani mwandishi wala shahidi. Na mkifanya hivyo basi hakika hilo ni kosa kwenu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.²⁸²

277 Hakika wale wanao muamini Mwenyezi Mungu, na wakazitimiza amri zake, na wakatenda mema aliyo waamrisha, na wakaacha yaliyo katazwa ya haramu, na wakatimiza Sala kwa njia ya ukamilifu, na wakatoa Zaka kuwapa wanao stahiki, watapata thawabu kubwa mno walio wekewa kwa Mola wao. Na wala hawatakuwa na khofu ya chochote kwa siku zijazo, wala hawatahuzunika kwa lolote walilo likosa.

278 Enyi mlio amini! Mwigopeni Mwenyezi Mungu, na wacheni heba yake na khofu yake ijae katika nyoyo zenu, na wacheni kudai hiyo riba iliyo bakia juu ya shingo za watu ikiwa ni kweli nyinyi ni Waumini.

279 Ikiwa hamfanyi aliyo kuamrisheni Mwenyezi Mungu kuacha riba basi kuweni na yakini kuwa nyinyi mko vitani na Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa sababu ya inadi yenu kuipinga amri ya Mwenyezi Mungu. Ikiwa mnataka toba ya kukubaliwa basi haki yenu ni kuchukua ile rasilmali yenu tu. Msichukue kitu zaidi, kidogo au kingi, bila ya kujali sababu ya hilo deni na vipi lilivyo tumiwa. Kwani hiyo ziada mnayo ichukua ni kumdhulumu mtu, kama vile kuacha sehemu ya rasilmali yenu ni dhulma juu yenu.

280 Ikiwa mwenye kukopeshwa ana shida na uzito basi mpeni muhula wa kulipa deni lake mpaka wakati wa kufarijika. Na mkitoa sadaka kwa kusamehe deni au baadhi yake ni kheri yenu kama nyinyi ni watu wenye ujuzi na fahamu kuelewa maneno ya Mwenyezi Mungu anaye kufundisheni murwa na utu.

281 Na ogopeni vitisho vya Siku mtao rejea kwa Mwenyezi Mungu, itapo kuwa kila nafsi italipwa kwa ililo tenda, ikiwa kheri au shari.

282 Enyi mlio amini! Mkiopeshana deni kwa muda, inatakikana huo muda ujuulikane. Nanyi muandikiane ili kuhifadhi haki na usitokee mzozo. Na lazima mwenye kuandika awe mtu muadilifu katika uandishi wake. Wala muandishi asikatae kuandika, kwani hivyo ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya ilimu aliyo mfunza naye alikuwa haijui. Basi aandike lile deni kwa mujibu anavyo kubali yule mwenye kukopa. Naye huyo mwenye kukopa amwogope Mola wake Mlezi, asipunguze hata chembe katika deni lilio juu yake. Pindi akiwa mwenye kukopa hawezi kujiendesha, wala hayawezi mambo vilivyo, au ni mnyonge kwa udogo au ugonjwa au ukongwe, au akawa hawezi kuandikisha kwa ajili ya ububu au

283. Na mkiwa safarini na hamkupata mwandishi, yatosha kukabidhiwa rahani. Na mmoja wenu akimwekea amana mwenziwe basi aliye aminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi. Wala msifiche ushahidi. Na atakaye ficha basi hakika moyo wake ni wenye kutenda dhambi. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mnayo yatenda.²⁸³

284. Viliomo mbinguni na viliomo duniani ni vya Mwenyezi Mungu. Na mkidhihirisha yaliyomo katika nafsi zenu au mkayaficha, Mwenyezi Mungu atakuhisabuni kwayo. Kisha amsamehe amtakaye na amuadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.²⁸⁴

285. Mtume ameamini yaliyo teremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake na Mitume wake. Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume wake, na (Waumini) husema: Tumesikia na tumet'ii. Tunakutaka maghfira Mola Mlezi wetu! Na marejeo ni kwako.²⁸⁵

286. Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyho. Faida ya iliyo yachuma ni yake, na khasara ya iliyo yachuma ni juu yake pia. (Ombeni:) Mola

uzito wa ulimi au kutojua lugha inayo andikiwa huo waraka, basi mlinzi wake wa kisharia au hakimu au aliye mkhiari yeye, awe ndiye naibu wake wa kutoa imla ya kuliandika hilo deni kwa uadilifu ulio timia. Na washuhudisheni deni hilo wanaume wawili miongoni mwenu. Ikiwa hawakupatikana wanaume wawili, basi mwanamume mmoja na wanawake wawili, washuhudie ili pindi mtu akirusha waweze kutoa ushahidi wao, na akisahau mmoja mwengine aweze kumkumbusha. Wala haijuzu kujuziua kutoa ushahidi pindi unapo takikana. Wala msipuuzie kuandika kidogo na kikubwa maadamu ni deni la kulipwa baadae. Hivyo ndio uadilifu wa sharia ya Mwenyezi Mungu, na ndio kuwa na nguvu zaidi kuwa ni dalili ya ukweli wa ushahidi, na ndio vyema zaidi kuondoa shaka shaka baina yenu. Ila ikiwa jambo lenyewe ni biashara ya mkono-kwa-mkono mnayo uzuiana baina yenu, hapo si lazima kuandikiana, kwani hapana dharura ya hayo. Na inatakikana lakini katika kuuziana pawepo mashahidi ili kuepusha ugomvi. Na tahadharini asipate madhara yoyote mwenye kuandika au mwenye kushuhudia. Hayo itakuwa ni kutokana na ut'iifu wa Mwenyezi Mungu. Na mkhofuni Mwenyezi Mungu, na ogopeni heba yake katika anayo amrisha na anayo yakataza. Hivyo ndio nyoyo zenu zitalazimika kufuata insafu na uadilifu. Na Mwenyezi Mungu anakubainishieni haki zenu na waajibu ulio juu yenu. Naye ni Mjuzi wa kila kitu - vitendo vyenu na vinginevyo. (*Tazama maelezo 2:282*)

283 Ikiwa mko safarini na hamkupata mtu wa kuliandika deni, basi kwa dhamana ya deni wekeni kitu kuwa ni rahani ashike mwenye kukopesha kutokana na mwenye kukopa. Na mtu akipewa dhamana na mwenzie kushika, basi iwe hiyo ni amana ilioko mikononi mwake. Yeye ametegemewa kwa uaminifu wake. Basi inapo takikana amana na aitoe amana ya watu. Na amche Mwenyezi Mungu aliye muumba na kumlea na kumshughulikia kwa uangalifu ili isimkatikie neema ya Mola wake Mlezi duniani na Akhera. Wala msifiche ushahidi unapo takikana. Mwenye kuficha amepata dhambi, na khabithi wa moyo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua mnayo yafanya. Atakulipeni kwa mujibu mnavyo stahiki.

284 Jueni kuwa vyote viliomo mbinguni na duniani ni vya Mwenyezi Mungu, naye ana makdara navyo vyote na anavijua vyote. Ni sawa sawa ikiwa mtadhihirisha yaliyomo ndani ya nafsi zenu au mkificha, Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa vyote na mwenye kupata khabari za vyote. Naye Siku ya Kiyama atakuhisabuni kwa hayo, na atamghufiria amtakaye na amuadhibu amtakaye. Yeye ni Muweza wa kila kitu.

285 Hakika aliyo teremshiwa Mtume Muhammad s.a.w. ni Haki itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Naye amemuamini Mwenyezi Mungu, na pamoja naye wameamini pia Waumini, wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake. Wao wanawaamini Mitume wote wa Mwenyezi Mungu sawa sawa, na wanawatukuza sawa, huku wakisema: Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume wake. Na wametilia mkazo Imani yao ya moyoni kwa kauli yao ya ulimini huku wakimuelekea Mwenyezi Mungu kumwambia: Mola Mlezi wetu! Tumesikia uliyo yateremsha yenye hikima, na tumeyapokea yaliyo amrisha. Ewe Mola wetu Mlezi! Tupe maghfira yako. Na kwako Wewe tu pekee ndio tunako kwendea na ndio marejeo.

Sura 2 - Al-Baqara

wetu Mlezi! Usituchukulie tukisahau au tukikosea. Mola wetu Mlezi! Usitubebeshe mzigo kama ulio wabebesha wale walio kuwa kabla yetu. Mola wetu Mlezi Usitutwike tusiyo yaweza, na utusamehe, na utughufirie, na uturehemu. Wewe ndiye Mlinzi wetu. Basi tupe ushindi tuwashinde kaumu ya makafiri.²⁸⁶

286 Hakika Mwenyezi Mungu hawakalifishi waja wake ila kwa kadiri wanavyo weza kuyafanya na kuyafuata. Kwa hivyo kila mwenye kukalifishwa atalipwa kwa vitendo vyake - akitenda kheri atapata malipo ya kheri, akitenda shari atapata shari. Basi enyi Waumini! Nyenyekeeni kwa Mwenyezi Mungu mkimuomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Usituadhibu pindi tukiporonyoka tukasahau ulio tuamrisha, au yakatupata ya kutusabibisha kutumbukia makosani. Mola Mlezi wetu! Usituchukulie kwa shida ukatupa sharia nzito nzito kama ulivyo wafanyia Mayahudi kwa sababu ya inda yao na udhalimu wao. Wala usitukalifishe mambo tusiyo yaweza, na utusamehe kwa ukarimu wako, na tughufirie kwa fadhila yako, na uturehemu kwa rehema yako yenye wasaa. Hakika Wewe ni Mola Mlezi wetu. Tunusuru ewe Mola Mlezi, kwa ajili ya kutukuza Neno lako na kuitangaza Dini yako - tuwashinde kaumu ya wapingaji.

Sura 3 - Al I'mran

Utangulizi

MIONGONI mwa mambo inayo yazungumzia Qur'ani ni hadithi za ada ya Mwenyezi Mungu katika uumbaji wake, na mifano na mazingatio yanayo patikana katika hizo hadithi. Na hubainisha katika hadithi hizo mambo mengi yaliyo khusu itikadi, hukumu za sharia na nyendo njema. Katika Sura iliyo pita yametajwa mfano wa mwendo wa Wana wa Israili. Yameelezwa mengi ya walivyo kengeuka. Na katika Sura hii yanatajwa mengine ya upotovu wao na kukengeuka kwao, na vipi Muumini anatakikana aongoke katika itikadi yake na mwenendo wake, na pia unabainishwa humu ukweli wa Dini ya Mbinguni, na inaonyeshwa vipi ziwe adabu za kujadiliana, na zinaelezwa ada za wakati wa kushinda na pengine wakati wa kushindwa. Pia inabainishwa vipi watakuwa wanao kufa Mashahidi Siku ya Kiyama, na yepi malipo yao. Na hayo yote kwa wanaume na wanawake. Na inaelezwa kadhaalika njia ya mafanikio. Sura hii tukufu inaanza kama ilivyo anza iliyo tangulia.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

1. Alif Laam Miim.¹
2. Mwenyezi Mungu, hakuna mungu ila Yeye Aliye Hai, Msimamizi wa yote milele.²
3. Amekuteremshia Kitabu kwa haki, kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati na Injili.³
4. Kabla yake, ziwe uwongofu kwa watu. Na akateremsha Furqani (Upambanuo). Hakika walio zikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu watakuwa na adhabu kali. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kulipa.⁴
5. Hakika Mwenyezi Mungu hakifichiki chochote kwake, duniani wala mbinguni.⁵
6. Yeye ndiye anaye kuundeni ndani ya matumbo ya wazazi kwa namna apendayo.

1 "Alif Laam Miim", yaani "A.L.M." ni harufi za kutamkwa na kusikilizana kwa sauti. Zimeletwa kubainisha kuwa hii Qur'ani ya miujiza imetokana na hizi hizi harufi zinazo tamkwa, ili watu watanabahi na wasikilize.

2 Mwenyezi Mungu ni Mmoja, hapana mungu isipo kuwa Yeye. Na kila kiliomu ulimwenguni kinashuhudia hayo kwa namna ya kilivyo umbika na kushikamana, katika umbo na kazi, na viumbe vyenginevyo. Na Yeye Mwenyezi Mungu ni Yuhai, hafi. Ni Mwenye kusimamia na kuendesha mambo yote ya ulimwengu. Yeye ndiye Mwenye kuyadabiri na kuyasarifu.

3 Umeteremshiwa wewe, Muhammad, hii Qur'ani yenye kukusanya ukweli wa misingi yote ya Sharia ya Mbinguni iliomo katika Vitabu vilivyo tangulia. Na hakika kabla ya Qur'ani Mwenyezi Mungu alikwisha teremsha Taurati kwa Musa, na Injili kwa Isa.

4 Ameziteremsha hizo kabla ya Qur'ani ili kuwaongoa watu. Walipo kengeuka akateremsha Qur'ani ipambanue baina ya Haki na baat'ili, baina ya kweli na uwongo, baina ya uwongofu na upotovu. Basi hii Qur'ani ni Kitabu cha kweli, chenye kudumu milele. Na kila mwenye kuacha aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu na akazikanya Aya zake, Ishara zake, atapata adhabu iliyo kali. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza, hashindwi na kitu, na Mwenye kuwalipa wanao stahiki kulipwa.

5 Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. Kwa hivyo hapana kinacho fichika kwake katika ardhi na hata katika mbingu, kikiwa kidogo au kikubwa, kinacho onekana na kisicho onekana.

Hapana mungu ila Yeye, Mwenye nguvu na Mwenye hikima.⁶

7. Yeye ndiye aliye kuteremshia Kitabu hichi. Ndani yake zimo Aya muhkam, zenye maana wazi. Hizo ndizo msingi wa Kitabu hichi. Na ziko nyengine za mifano. Ama wale ambao nyoyoni mwao umo upotovu wanafuata zile za mifano kwa kutafuta fitna, na kutafuta maana yake; na wala hapana ajuaye maana yake ila Mwenyezi Mungu. Na wale wenye msingi madhubuti katika ilimu husema: Sisi tumeziamini, zote zimetoka kwa Mola wetu Mlezi. Lakini hawakumbuki hayo isipo kuwa wenye akili.⁷

8. (Na hao husema): Mola wetu Mlezi! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kwisha tuongoa, na utupe rehema itokayo kwako. Hakika Wewe ndiye Mpaji.⁸

9. Mola wetu Mlezi! Wewe ndiye Mkusanyaji wa watu kwa Siku isiyo na shaka ndani yake. Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi yake.⁹

10. Kwa hakika wale walio kufuru hazitowafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu mali zao, wala watoto wao; nao hao ndio kuni za Motoni-¹⁰

11. - Kama yaliyo wapata watu wa Firauni na wale walio kuwa kabla yao. Walikanusha Ishara zetu, basi Mwenyezi Mungu aliwashika kwa madhambi yao; na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.¹¹

12. Waambie walio kufuru: Karibuni mtashindwa na mtakusanywa, mtiwe kwenye Jahannam; nako huko ni makao mabaya kabisa.¹²

13. Hakika ilikuwa ni Ishara kwenu katika yale majeshi mawili yalipo pambana. Jeshi moja likipigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na jingine kafiri likiwaona zaidi kuliko wao mara mbili, kwa kuona kwa macho. Na Mwenyezi Mungu humuunga mkono amtakaye kwa nusura yake. Hakika katika hayo yapo mazingatio kwa wenye

6 Ni Yeye, Mwenyezi Mungu, ndiye anakuundeni, anakupeni Sura na hali nyinyi mmo matumboni mwa mama zenu, kwa Sura na umbo mbali mbali kama apendavyo Yeye. Hapana mungu ila Yeye Mwenye nguvu katika ufalme wake, Mwenye hikima katika kuunda kwake.

7 Na Yeye Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuteremshia wewe, Muhammad, hii Qur'ani. Na ni katika hikima yake kufanya ndani yake mna Aya zilizo wazi, maana yake na makusudio yake yanajuulikana wepesi. Hizi ndio msingi, ndio asli. Marejeo yote yawe juu ya hizi. Na zipo Aya nyengine za mifano, za mshabaha, zenye kutatanisha. Wengi hawawezi kuzielewa. Na wale ambao hawakubobea, hawakuzama katika ilimu, huwababaisha. Na zimeteremka hizi Aya za mifano ili wanazuoni wachungue kutafuta ilimu ndani yake, na wazingatie, na wazidi kufikiri katika jitihadi, na kufanya uchunguzi katika Dini. Lakini mtindo wa walio iacha Haki ni kutaka kuzifuata hizo Aya za mifano ili kutaka kuchochea fitna, na huzifasiri kwa kufuata matamania yao. Na hapana anaye jua maana ya Aya hizi kwa hakika ila Mwenyezi Mungu, na wale walio thibiti kweli katika ilimu. Na hao walio thibiti husema: "Sisi tuna yakini kuwa hayo yanatokana na Mwenyezi Mungu. Sisi hatufarikishi katika kuiamini Qur'ani baina ya sehemu zilizo wazi (Muhkam) na zile za mifano (Mutashaabih). Na hawazingatii ila watu wenye akili iliyo nzima, ambayo haifuati pumbao na matamania.

8 Hao wanazuoni wenye akili husema: Mola wetu Mlezi! Usizifanye nyoyo zetu zikaacha Haki baada ya Wewe kwisha tuongoza kuiendea hiyo Haki. Ewe Mola wetu Mlezi! Tupe rehema kutoka kwako kwa kutuwezesha na kututhibitisha. Hakika Wewe ndiwe Mwenye kunyima na ndiwe Mpaji.

9 Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ndiwe utao wakusanya watu Siku hiyo isiyo na shaka, ili kumlipa kila mmojapo kwa alilo litenda. Kwani Wewe umeahidi hayo, na Wewe hukhalifu miadi yako.

10 Katika Siku hiyo makafiri hawatokingwa na mali yao na yangawa mengi vipi, wala na watoto wao na wangawa wengi vipi. Hayo yote yatakuwa ndio kuni za Moto za kuwateketeza wenyewe

11 Na hali ya hao ni kama hali ya kaumu ya Firauni walio kuwa na inda kabla yao. Walizikadhibisha Ishara za Mwenyezi Mungu juu ya kuwa zilikuwa ziwazi kabisa. Basi Mwenyezi Mungu akawaadhibu kwa sababu ya madhambi waliyo yatenda. Na Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.

12 Ewe Nabii! Waambie hawa walio kufuru: Bila ya shaka nyinyi mtashindwa hapa duniani, na kesho Akhera mtaadhibiwa. Na Jahannamu ndio itakuwa tandiko lenu la kulalia; na ovu lilioje tandiko hilo!

macho.¹³

14. Watu wamepambiwa kupenda matamaniao ya wanawake, na wana, na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi asili, na mifugo, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema.¹⁴

15. Sema: Nikwambieni yaliyo bora kuliko hayo? Kwa wachamngu ziko Bustani kwa Mola wao zipitazo mito kati yake. Watadumu humo, na wake walio takaswa, na wanazo radhi za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona waja wake,¹⁵

16. Ambao husema: Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumeamini, basi tufutie madhambi yetu, na tuesushe na adhabu ya Moto,¹⁶

17. Wanao subiri, wanao sema kweli, na wat'iifu, na wanao toa sadaka, na wanao omba maghafira kabla ya alfajiri.¹⁷

18. Mwenyezi Mungu, na Malaika, na wenye ilimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana mungu ila Yeye, ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana mungu ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye hikima.¹⁸

19. Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu. Na walio pewa Kitabu

13 Ilikuwa Ishara wazi na mazingatio yaliyo dhaahiri katika makundi mawili ya wapiganaji walipo pambana siku ya Badri. Kundi moja, hilo la Waumini, likipigana kwa ajili ya kutukuza Neno la Mwenyezi Mungu na kueneza Haki. Na kundi la pili, hilo la makafiri, likipigania pumbao na matamaniao. Ikawa, basi, Mwenyezi Mungu katika kuwaunga mkono Waumini aliwafanya wale makafiri wawaone Waumini idadi yao mara mbili kuliko walivyo. Kwa hivyo makafiri wakaingiwa na khofu nyoyoni mwao wakaemewa. Na Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Katika haya, hakika, pana mazingatio kwa wenye nadhari iliyo ongoka isiyo kengeuka na kuiacha Haki.

14 Wanaadamu wameumbwa kuwa wanapenda matamaniao ya vitu kama wanawake, wana, na wingi wa madhahabu na fedha, na farasi wazuri wazuri walio fundishika, na mifugo kama ngamia, ng'ombe, mbuzi, kondoo, na kadhaalika mashamba makubwa. Lakini yote hayo ni starehe na kwa matumizi ya uhai huu wa duniani wenye kupita na kuondoka. Na hayo si chochote si lolote ukilinganisha na hisani anayo wafanyia Mwenyezi Mungu waja wake wanao pigania jihadi katika Njia yake watakapo rejea kwake Yeye Akhera

15 Ewe Nabii! Sema: Nikwambieni yaliyo bora kuliko hayo yote mliyo pambiwa duniani? Kwa wale wachamngu wamewekewa malipo ya dhamana kwa Mola wao Mlezi, nayo ni Bustani zipitazo mito chini ya vivuli vya miti. Humo watastarehe kwa maisha mazuri wala hawatoingiliwa na khofu ya kuwa neema hiyo itaondoka, kwani wamekwisha katibiwa kuwa humo watabaki daima milele. Watakuwamo humo wake walio t'ahirika, wamesafika na kila ila ya wanawake wa kidunia. Na juu ya yote hayo, watapata Radhi ya Mwenyezi Mungu ambayo wataihisi chini ya kivuli chake kuwa ndiyo Neema kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu anazijua vyema hali za waja wake; hapana jambo linalo fichikana kwake, hawana siri asiyo ijua Yeye.

16 Malipo haya watayapata wale ambao nyoyo zao zimejaa Imani, na wakatangaza kwa ndimi zao wakisema kwa kumnyenyekea Mwenyezi Mungu: Mola Mlezi wetu! Hakika sisi tumeamini kwa kuitikia wito wako. Basi tusamehe dhambi zetu, na utuhifadhi na adhabu ya Moto.

17 Na malipo haya huyapata wanao stahamili mashaka kwa ajili ya ut'iifu wao, na kujitenga na maasi, na kuvumilia dhiki, watu ambao ni wakweli katika kauli zao na vitendo vyao, na niya zao, wenye kudumu katika ut'iifu kwa kunyenyekea, wenye kutoa wawezacho bilhali walmali na vyenginevyo kwa sababu ya mambo ya kheri, ambao kwamba wanamtaka msamaha Mwenyezi Mungu mwishoni mwa usiku, kabla ya alfajiri, zinapo safika roho na hutengenea kuzingatia na kutafakari katika utukufu wa Muumbaji.

18 Mwenyezi Mungu amebainisha wazi katika maumbaji yake dalili na Ishara ambazo hawezi kuzipinga mwenye akili, ya kwamba Yeye ni Mmoja, wala hana mshirika wake, na kwamba Yeye ndiye Mwenye kusimamia mambo ya viumbe vyote kwa uadilifu. Na kwa haya pia wamekiri Malaika walio t'ahirika, na wameyajua watu wa ilimu kwa yakini, na kwamba Yeye ilio tukuka shani yake ni Mpweke katika Ugu, wala hana wa kumshinda katika jambo, na hikima yake imeenea kila kitu.

hawakukhitalifiana ila baada ya kuwajia ujuzi, kwa sababu ya uhasidi ulio kuwa baina yao. Na anaye zikataa Ishara za Mwenyezi Mungu basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.¹⁹

20. Na pindi wakikuhaji, basi sema: Mimi nimeusalimisha uso wangu kumwelekea Mwenyezi Mungu, na kadhaalika walio nifuata. Na waambie walio pewa Kitabu na wasio na kisomo: Je! Mmesilimu? Wakisilimu basi wameongoka. Na wakikengeuka basi juu yako ni kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona waja wake.²⁰

21. Hakika wanao zikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakawauwa Manabii pasipo haki, na wakawauwa watu waamrishao Haki wabashirie adhabu kali.²¹

22. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika duniani na Akhera. Nao hawatapata wa kuwanusuru.²²

23. Huwaoni wale walio pewa sehemu ya Kitabu? Wanaitwa kukiendea Kitabu cha Mwenyezi Mungu ili kiwahukumu baina yao; kisha baadhi yao wanageuka wanakikataa.²³

24. Hayo ni kwa sababu walisema: Hautatugusa Moto isipo kuwa kwa siku chache tu. Na yakawadanganya katika dini yao yale ambayo wenyewe waliyo kuwa wakiyazua.²⁴

25. Basi itakuwaje tutakapo wakusanya Siku ambayo haina shaka kuja kwake? Na kila nafsi italipwa kama ilivyo chuma, bila ya kudhulumiwa.²⁵

26. Sema: Ewe Mwenyezi Mungu uliye miliki ufalme wote! Wewe humpa ufalme umtakaye, na humwondolea ufalme umtakaye, na humtukuzwa umtakaye, na

19 Hakika Dini ya Haki aliyo iridhi Mwenyezi Mungu ni Dini ya Tawhidi, ya Mungu Mmoja, na kumnyenyekea Yeye kwa usafi wa moyo. Mayahudi na Wakristo wamekhitalifiana na Dini hii, wakazua na wakabadilisha. Na wala kukhalifu kwao hakukuwa kwa kudanganyikiwa au kwa ujinga ilipo wajia ilimu, bali yalikuwa hayo kwa uhasidi na ushindani tu. Na mwenye kupinga Ishara za Mwenyezi Mungu, basi na angojee hisabu ya Mwenyezi Mungu, nayo yenda kasi mno.

20 Na hawa makafiri wakijadiliana nawe katika Dini hii baada ya wewe kuwapa hoja zote, huna haja kupigizana nao kelele kwa majadiliano. Waambie tu: Mimi na Waumini walio nifuata tumemsafia Mwenyezi Mungu peke yake ibada yetu. Na waambie Mayahudi na Wakristo na washirikina wa Kiarabu: Dalili zimekwisha bainika kwenu, basi silimuni. Wakisilimu inakuwa wameijua njia ya uwongofu na wameifuata. Na wakikataa huna lawama wewe kwa kukataa kwao. Waajibu wako ni kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu tu. Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema waja wake. Hapana lolote lao, hali yao na vitendo vyao, linalo fichikana kwake.

21 Hakika wale wanao zipinga Ishara za Mwenyezi Mungu katika uumbaji na hizi zilizo teremka, na wakawauwa Manabii alio watuma Mwenyezi Mungu waje kuwaongoa - bila ya haki kabisa, na hiyo ni dhulma kubwa mno - na wakawauwa wale wanao waita watu wafanye haki na uadilifu, watu hao wanastahiki adhabu kali. Basi wabashirie adhabu hiyo!

22 Watu wenye sifa kama hizo, a'mali zao zimebat'ilika ijapo kuwa baadhi yake ni njema, na hazina matunda. Kwa hivyo haziwafai duniani, na mwisho wake ni hizaya na adhabu huko Akhera. Na wala hawana wa kuwaokoa na khasara na adhabu watayo ipata.

23 Je! Huijui hali ya wale walio pewa sehemu ya Kitabu na ilimu (nao ni Mayahudi na Wakristo) wanaitwa wende kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu, nacho ni Qur'ani ili kiwapambanulie baina ya Kweli na uwongo, Haki na baat'ili, katika khitilafu zilizo zuka baina yao, na wala hawafanyi haraka ya kumuitikia anaye waita. Bali baadhi yao wanamkataa; shani yao ni kuukataa wito wa kheri.

24 Hao wanao kataa miongoni mwa Mayahudi wamedanganyika kwa kukataa kwao na matumaini ya uwongo wanao jitamanisha nafsi zao ya kuwa Moto hautawagusa ila siku chache tu. Na kudanganyika huko na matamainio hayo yamewapelekea kuendelea kuzua katika dini yao kunako endelea.

25 Basi itakuwaje hali yao wakati atapo wakusanya Mwenyezi Mungu Siku ya Akhera, ambayo hapana shaka kuwapo kwake, na kuwa kutakuwapo kuhisabiwa. Basi kila nafsi itapewa malipo yake ya kutosha. Na wao wanastahili kupata hiyo adhabu ya Jahannamu watakayo ipata.

humuangusha umtakaye. Kheri yote iko mikononi mwako. Hakika Wewe ni Muweza wa kila kitu.²⁶

27. Wewe huingiza usiku katika mchana, na huingiza mchana katika usiku. Na humtoa hai kutokana na maiti, na humtoa maiti kutokana na aliye hai. Na unamruzuku umtakaye bila ya hisabu.²⁷

28. Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anaye fanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu anakuhadharisheni naye. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.²⁸

29. Sema: Mkiyaficha yaliyomo vifuani mwenu au mkiyafichua Mwenyezi Mungu anayajua; na anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo duniani. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.²⁹

30. Siku ambayo kila nafsi itakuta mema iliyo yafanya yamehudhurishwa, na pia ubaya ilio ufanya. Itapenda nafsi lau kungekuwako masafa marefu baina ya ubaya huo na yeye. Na Mwenyezi Mungu anakuhadharisheni naye. Na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake.³⁰

31. Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi

26 Ewe Nabii! Sema kwa unyenyekevu na kuukiri utukufu wake Mwenyezi Mungu: Ewe Mola Mlezi! Ni Wewe peke yako ndiye Mwenye kumiliki kutasarafu katika mambo yote. Unampa kuhukumu na utawala umtakaye, na unamnyima umtakaye. Unampa utukufu umpendaye kati ya waja wako kwa kumwezesha kuzishika sababu za kuufikia huo utukufu. Na unampiga madhila na unyonge umtakaye. Basi Wewe peke yako unamiliki kheri yote. Hushindwi na kitu katika kutimiza muradi wako na yanayo kupelekea hikima yako kuyakatia shauri katika mipango ya uumbaji wako.

27 Na Wewe kwa ulivyo umbwa na ukawekea sababu na nyendo, unauingiza usiku katika mchana kwa unavyo zidi mchana urefu wake, na unauingiza mchana katika usiku kwa unavyo zidi usiku urefu wake. Na unatoa chenye sifa za kuonekana kihai katika kisicho kuwa na sifa za uhai, kama unavyo toa chenye kukosa uhai kutokana na kilicho hai, chenye kutamakani na sababu za uhai. Unampa neema zako kubwa umtakaye kwa mujibu wa mipango ya hikima zako. Hapana mchunguzi wa kukuhisabu Wewe. Huyu Mwenye shani hii haemewi na kumjaalia Mtume wake na awapendao, ubwana, na utawala, na utajiri, na wasaa, kama alivyo waahidi.

28 Ikiwa basi ni Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* ndiye Yeye peke yake Mmiliki wa mamlaka, anatukuza na kuangusha, na katika mikono yake pekee ipo kheri, na uumbaji, na riziki, basi haifai kwa Waumini kuwafanya wasio kuwa Waumini wawe na utawala juu yao, wakauwacha msaada wa Waumini wenzao. Kwani wakifanya haya inakuwa wanaivunja Dini, na wanawaletea maudhi wenye Dini, na ni kuudhoofisha utawala na udugu wa Kiislamu. Na mwenye kufuata njia hii basi kwa Mwenyezi Mungu Mmiliki wa mamlaka yote hana lake jambo. Wala haimfalii Muumini kuridhia kuwapa utawala na ulinzi makafiri ila awe hana hila. Hapo basi anaweza kujikinga na madhara yao kwa kuonyesha ut'ifu kwao. Ni juu ya Waumini wawe daima katika ulinzi wa Kiislamu, kwani huo ndio ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Na watahadhari wasitoke kwenye ulinzi wa Mwenyezi Mungu kuuendea ulinzi mwengine asije akawaadhibu kwa kuwaletea madhila baada ya utukufu. Na kwake Yeye ndio marejeo, wala hapana pa kukimbilia kutokana na madaraka yake duniani wala Akhera.

29 Sema, ewe Nabii! Mkiyaficha yaliyomo vifuani mwenu au mkiyadhihirisha katika vitendo vyenu na kauli zenu ni sawa, kwani Mwenyezi Mungu anayajua yote, na anayajua yote yaliyomo mbinguni na yaliyomo duniani, yanayo onekana na yanayo fichikana. Uwezo wake unapenya katika viumbe vyake vyote.

30 Basi na watahadhari wale wanao ikhalifu amri yake na Siku ambayo kila mtu atakuta vitendo vyake vya kheri hata kilicho kichache kimeletwa hadharani; na pia uovu wake alio utenda ambao angetamani lau kuwa uko mbali, mwisho wa umbali, hata asiune kwa kuuchukua na kukhofu kutumbukia katika adhabu zake. Na Mwenyezi Mungu anakuhadharisheni na adhabu zake pindi mkitokana na ulinzi wake na utawala wake, ambao ni upole na rehema kwa waja wake.

Sura 3 - Al I'mran

Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu.³¹

32. Sema: Mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakigeuka basi Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri.³²

33. Hakika Mwenyezi Mungu alimteua Adam na Nuhu na ukoo wa Ibrahim na ukoo wa Imran juu ya walimwengu wote.³³

34. Ni wazao wao kwa wao; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua.³⁴

35. Alipo sema mke wa Imran: Mola wangu Mlezi! Nimekuwekea nadhiri kilichomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Hakika Wewe ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.³⁵

36. Basi alipo mzaa alisema: Mola wangu Mlezi! Nimemzaa mwanamke - na Mwenyezi Mungu anajua sana aliye mzaa - Na mwanamume si sawa na mwanamke. Na mimi nimemwita Maryamu. Nami namkinga kwako, yeye na uzao wake, uwalinde na Shet'ani aliye laaniwa.³⁶

37. Tena Mola wake Mlezi akampokea kwa mapokeo mema na akamkuza makuzo mema, na akamfanya Zakariya awe mlezi wake. Kila mara Zakariya alipo ingia chumbani kwake alimkuta na vyakula. Basi alimwambia: Ewe Maryamu! Unavipata wapi hivi? Naye akasema: Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.³⁷

31 Sema: Ikiwa nyinyi ni wakweli katika madai yenu, kuwa mnampenda Mwenyezi Mungu na mnataka Mwenyezi Mungu akupendeni, basi nifuateni mimi kwa ninayo kuamrisheni na ninayo kukatazeni. Kwani mimi nimetumwa na Mwenyezi Mungu. Basi Mwenyezi Mungu atakupendeni kwa hivyo, na atakulipeni kwa kukufanyieni hisani na kusamehe makosa yenu. Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kuwasamehe na kuwarehemu waja wake.

32 Sema: Mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakikukataa basi hao ni makafiri, wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri.

33 Kama Mwenyezi Mungu alivyo mteua Muhammad afikishe ujumbe wake, na akajaalia kumfuata Muhammad ni njia ya kufikia mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kupata maghfira na rehema yake, kadhaalika ametaja Mwenyezi Mungu kuwa Yeye alimteua Adam na akamjaalia ni katika wateule wa walimwengu. Pia alimteua Nuhu kwa kumpa ujumbe, na akamteua Ibrahim na ukoo wake, nao ni Ismail na Is-haq na Manabii wengine kutokana na wana wao hao. Miongoni mwao ni Musa a.s. *Akawakhitari* ukoo wa Imran, na miongoni mwao akamkhitari Isa na mama yake. Alimfanya Isa awe ni Mtume kwa Wana wa Israili, na Maryam akamfanya awe ni mama wa Isa bila ya baba.

34 Amewakhitari hao ukoo ulio safi, wakirithiana usafi na fadhila na kheri. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia maneno ya waja wake kwa vitendo vyao na vinavyo fichwa vifuani mwao.

35 Ewe Nabii! Taja hali ya mke wa Imran alipo weka nadhiri wakati alipo kuwa na mimba, kuwa mwana aliomo tumboni mwake awe ni wa kumtumikia Mwenyezi Mungu tu na kukhudumia nyumba yake. Alisema: Ewe Mola! Hakika mimi nimekuwekea nadhiri huyu aliyomo tumboni mwangu awe ni wa kukhudumia nyumba yako, basi nikubalie haya. Hakika Wewe ni Mwenye kusikia kila kauli, na Mwenye kujua kila hali.

36 Alipo jifungua mimba akasema kwa kujiudhuru kumwambia Mola wake Mlezi: Niliye mzaa ni mwanamke - na Mwenyezi Mungu anajua vilivyo alichu kizaa, na kuwa mwana wenyewe ni mwanamke ni bora kuliko alivyo taka mama kuwa awe mwanamume. Akasema yule mama: Mimi nimemwita Maryamu, na mimi nakuomba umlinda yeye na ukoo wake na uharibifu wa Shetani maluuni.

37 Mwenyezi Mungu alimpokea Maryamu kuwa ni nadhiri aliyo iweka mama yake, akamwitikia maombi yake, akamkuza makuzo mema, na akamlea katika kheri yake, Mola Mlezi, huku akimruzuku na kumshughulikia kwa malezi mazuri ya kumpa nguvu mwili wake na roho yake. Mwenyezi Mungu akamkabidhi Zakariya a.s. awe mlezi wake. Zakariya kila akiingia chumbani, alipo kuwa Maryamu anaabudu, akikuta chakula wasicho kizowea wakati ule. Zakariya akasema kwa kustaajabu: Ewe

- 38.** Pale pale Zakariya akamwomba Mola wake Mlezi, akasema: Mola wangu Mlezi! Nipe kutoka kwako uzao mwema. Wewe ndiye unaye sikia maombi.³⁸
- 39.** Alipo kuwa kasimama chumbani akisali, Malaika kamnadia: Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria Yahya, ataye kuwa mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu, na ni bwana na mt'awa na Nabii kwa watu wema.³⁹
- 40.** Akasema Zakariya: Mola wangu Mlezi! Vipi nitapata mwana na hali ukongwe umenifikia, na mke wangu ni tasa? Akasema: Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo.⁴⁰
- 41.** Akasema: Mola wangu Mlezi! Niwekee alama. Akasema: Alama yako ni kuwa hutasema na watu kwa siku tatu, isipo kuwa kwa kuashiria tu. Na mdhukuru Mola Mlezi wako kwa wingi na mtakase jioni na asubuhi.⁴¹
- 42.** Na angalia pale Malaika walipo sema: Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amekuteuwa, na akakutakasa, na akakutukuza kuliko wanawake wote.⁴²
- 43.** Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola Mlezi wako na usujudu na uiname pamoja na wainamao.⁴³
- 44.** Hizi ni khabari za ghaibu tunazo kufunulia; nawe hukuwa nao walipo kuwa wakitupa kalamu zao nani wao atamlea Maryamu, na hukuwa nao walipo kuwa wakishindana.⁴⁴
- 45.** Na pale Malaika walipo sema: Ewe Maryamu! Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria (mwana) kwa neno litokalo kwake. Jina lake ni Masihi Isa mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa walio

Maryamu! Umepata wapi riziki hii? Naye akamjibu: Hichi ni katika fadhila za Mwenyezi Mungu. Ni shani yake kumruzuku mja wake amtakaye riziki nyingi bila ya hisabu au kipimo.

38 Zakariya a.s. alipo iona neema ya Mwenyezi Mungu kwa Maryamu alimwelekea Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu akimwomba kwa fadhila yake na ukarimu wake na uwezo wake, naye ampe mtoto mwanamume. Kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia maombi ya mwenye kuomba kwake kwa unyenyekevu. Naye ni Muweza wa kuitikia maombi na hata zinge kuwapo pingamizi za kikawaida kama ukongwe na utasa.

39 Mwenyezi Mungu alitikia dua yake. Malaika akamnadia naye kasimama pahala pake pa ibada akimwelekea Mola wake Mlezi kumbashiria mtoto mwanamume jina lake Yahya, atakaye muamini Isa a.s. ambaye atazaliwa kwa kauli ya Mwenyezi Mungu kwa njia isiyo ya dasturi. Na Yahya atawahimiza kaumu yake kushika ilimu na kusali, na atakataza mambo ya pumbao na matamanio, na atamfanya awe miongoni mwa Manabii na watu wema.

40 Basi Zakariya alipo pewa bishara hii, ya kupata mwana, alimwelekea Mola Mlezi wake kwa shauku ya kutaka kujua vipi yatakuwa hayo, ya kuwa na mwana na ilhali yeye hanazo njia zijuulikanazo, kwa kuwa yeye mwenyewe kesho kongu, na mkewe ni tasa. Mwenyezi Mungu akamjibu kuwa Yeye anapo taka jambo ama huzileta njia au huumba bila ya njia zinazo juulikana. Kwani Yeye hutenda apendavyo.

41 Zakariya akamwomba Mola wake Mlezi amfanyie alama ya kuhakikisha bishara hii. Mwenyezi Mungu akamjibu: Alama yako ni kuwa hutaweza kusema na watu muda wa siku tatu, isipo kuwa utatumia ishara tu kuashiria utakacho. Na shikamana na dhikri ya Mwenyezi Mungu ukimtakasa na kumtukuza jioni na asubuhi.

42 Na kumbuka ewe Nabii, pale Malaika walipo mwambia Maryamu ya kwamba Mwenyezi Mungu amekukhitari uwe ni mama wa Nabii wake, na amekusafisha na kila uchafu, na amekuteuwa wewe uwe mama wa Isa kuliko wanawake wote wengineo.

43 Na kwa haya ewe Maryamu, yanakuwajibikia wewe umshukuru Mola wako Mlezi. Basi jilazimishe ut'iifu kwake, na uwe mwenye kushika Sala, na shirikiana na wengine wanao muabudu Mwenyezi Mungu na wanasali kwa ajili yake.

44 Haya unayo simuliwa wewe Muhammad na Qur'ani ni katika khabari tukufu za wale alio wateuwa Mwenyezi Mungu, nazo ni khabari za ghaibu ambazo Mwenyezi Mungu anakufunulia. Na wala wewe hukuwapo wakati walipo kuwa wakipiga kura kwa mishale, ili waweze kukata shauri juu ya Maryamu. Na wala wewe hukuwapo walipo gombana kuwania nani wa kupata cheo hicho kitukufu.

karibishwa (kwa Mwenyezi Mungu).⁴⁵

46. Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utuuzima wake, na atakuwa katika watu wema.⁴⁶

47. Maryamu akasema: Mola wangu Mlezi! Vipi nitampata mwana na hali hajanigusa mwanaadamu? Mwenyezi Mungu akasema: Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu huumba apendacho. Anapo hukumu jambo, huliambia: Kuwa! Likawa.⁴⁷

48. Na atamfunza kuandika na Hikima na Taurati na Injili.⁴⁸

49. Na ni Mtume kwa Wana wa Israili kuwaambia: Mimi nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu, ya kwamba nakuundieni kwa udongo kama sura ya ndege. Kisha nampuliza anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa na wakoma, na ninawafufua maiti kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninakwambieni mnacho kila na mnacho weka akiba katika nyumba zenu. Hakika katika haya ipo Ishara kwenu ikiwi nyinyi ni wenye kuamini.⁴⁹

50. Na ninasadikisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mlio harimishiwa, na nimekujieni na Ishara kutokana na Mola Mlezi wenu. Kwa hivyo mcheni Mwenyezi Mungu na nit'iini mimi.⁵⁰

51. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi na ni Mola wenu Mlezi. Basi

45 Kumbuka na utaje ewe Nabii, pale Malaika walipo mbashiria Maryamu kuwa atamzaa mwana kwa neno lake tu Mwenyezi Mungu kinyume na ada wanavyo zaliwa watu. Jina lake mwana huyo ni Masihi Isa bin Maryamu. Na Mwenyezi Mungu amemjaalia hapa duniani kuwa atakuwa na cheo kwa unabii wake na kuepukana na aibu zote, na kesho Akhera kuwa atakuwa na cheo cha juu pamoja na kundi la walio takasika, wakawa wenye kuwa karibu mno na Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii walio imara baraabara.

46 Na Mwenyezi Mungu alimjaalia Nabii Isa na uwezo wa kusema na watu na ilhali yungali mtoto maneno ya kufahamika yenye hikima, kama alivyo sema nao utuuzimani mwake, bila ya tafauti katika hali hizo mbili. Na akawa katika miongoni walio jaaliwa kuwa ni watu wema.

47 Maryamu alisema kwa kustaajabu kupata mwana kwa njia isiyo ya kawaida: Vipi nitapata mwana na ilhali hapana mwanamume aliyenigusa? (yaani aliye lala nami). Mwenyezi Mungu Mtukufu akakumbusha kuwa Yeye huumba atakacho kwa kudra yake bila ya shuruti za sababu zilizo zowewa. Kwani Yeye akitaka jambo hulileta tu kwa taathira ya uwezo wake katika atakalo bila ya kutafuta kinginecho cha kutimiza matakwa yake.

48 Na Mwenyezi Mungu atamfunza mtoto huyu aliye zaliwa kuandika, na ilimu njema yenye manufaa, na Taurati, Kitabu cha Musa a.s., na Injili atayo mfunulia yeye.

49 Na atamtuma awe Mtume wake kwa Wana wa Israili, (Katika Injili ya Mathayo 15.24 Yesu anasema: Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.- Tazama pia Mathayo 10.5-6 na Mathayo 19.28 na Yohana 17.9) mwenye kutumia hoja za ukweli wa Utume wake kwa miujiza kutokana na Mwenyezi Mungu. Miujiza yenyewe ni kama kufanya kwa udongo Sura ya ndege, kisha akipulizia vitaingia uhai na kutaharaki mithili ya ndege kwa atakavyo Mwenyezi Mungu. Pia ataponyesha, kwa kudra ya Mwenyezi Mungu, walio zaliwa vipofu na wataona, na wenye maradhi ya ukoma waondokewe na ukoma, na walio onekana wamekwisha kufa wafufuke. Na yote hayo ni kwa idhini na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Pia atawatajia wanacho weka akiba majumbani mwao, vyakula na vyenginevyo. Naye Nabii Isa awaambie: Ishara zote hizi Mwenyezi Mungu amezionyesha kwangu ili iwe hoja kuwa Utume wangu ni wa haki, ikiwa nyinyi ni katika watu wanao t'ii na kusadiki.(Katika Injili ya Yohana 5.30 Yesu anasema: Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe.)

50 Na mimi nimetumwa kwenu nisadikishe sharia ya Taurati aliyo teremshiwa Musa, na nikuhalalishieni, kwa amri ya Mwenyezi Mungu, baadhi ya mliyo harimishiwa zamani. Na mimi nimekuja na ishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuthibitisha ukweli wa ujumbe wangu. Basi mcheni Mwenyezi Mungu na nit'iini mimi.(Katika Injili ya Mathayo 5.17 Yesu anasema: Msidhani ya kuwa nilikuja kuitangua torati au manabii, la, sikuja kutangua, bali kutimiza.)

muabudni Yeye. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka.⁵¹

52. Isa alipo hisi kuwa kati yao pana ukafiri alisema: Nani wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu? Wanafunzi wake wakasema: Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu. Tumemuamini Mwenyezi Mungu, na shuhudia kwamba sisi hakika ni Waislamu.⁵²

53. Mola wetu Mlezi! Tumeyaamini uliyo yateremsha, na tumemfuata huyu Mtume, basi tuandike pamoja na wanao shuhudia.⁵³

54. Na Makafiri walipanga mipango na Mwenyezi Mungu akapanga mipango, na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa wenye kupanga.⁵⁴

55. Pale Mwenyezi Mungu alipo sema: Ewe Isa! Mimi nitakufisha, na nitakunyanyua kwangu, na nitakutakasa na wale walio kufuru, na nitawaweka wale walio kufuata juu ya wale walio kufuru, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu, nikuhukumuni katika yale mliyo kuwa mkikhitalifiana.⁵⁵

56. Ama wale walio kufuru, nitawaadhibu adhabu kali katika dunia na Akhera, wala hawatapata wa kuwanusuru.⁵⁶

57. Na ama wale walio amini na wakatenda mema basi Mwenyezi Mungu atawalipa ujira wao kaamili. Na Mwenyezi Mungu hawapendi madhaalimu.⁵⁷

58. Haya tunayo kusomea ni katika Aya na Ukumbusho wenye hikima.⁵⁸

59. Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam; alimuumba

51 Kwani hakika Mwenyezi Mungu ametumiminia mimi na nyinyi kila namna ya wema, amenilea mimi na nyinyi, ni Mola Mlezi wenu na wangu mimi. Basi muabuduni Yeye tu. Na hii ndio njia isiyo kwenda ovyo.

52 Basi alipo kuja Isa a.s. akawaita watu wake wafuate Njia Iliyo Nyooka, wengi wao walikataa. Alipo yajua hayo aliwaelekea na kuwaambia: Ni nani atakaye nisaidia katika kazi hii niifanyayo ya kuitia kwenye Haki? Wakamjibu baadhi ya Waumini wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na yeye: Sisi tunakuunga mkono, na tutakusaidia, kwa sababu wewe ni Mwitaji, unaita watu wende kwa Mwenyezi Mungu. Na shuhudia kuwa sisi tumemsafia Mwenyezi Mungu na ni wenye kufuata amri zake.

53 Na sisi tunasema: Ewe Mola Mlezi wetu! Tumekisadiki Kitabu chako ulicho mteremshia Nabii wako, na tunaifuata amri ya Mtume wako, Isa a.s. Basi tuthibitisha kuwa miongoni mwa wenye kumshuhudia Mtume wako katika kufikisha ujumbe, na kuwashuhudia Wana wa Israili katika ukafiri wao na upinzani wao.

54 Ama hao makafiri wapinzani walipanga njama za chini kwa chini kuupiga vita wito (Da'wa) wa Isa. Mwenyezi Mungu alizibat'ilisha njama zao, wasifanikiwe kuyapata waliyo yakusudia. Na Mwenyezi Mungu kwa hikima yake anawashinda watu wote wafanyao hila.

55 Taja ewe Nabii, pale Mwenyezi Mungu alipo sema: Ewe Isa Mimi nitakutumizia ajali yako, (yaani nitakufisha kifo cha kawaida kama alivyo sema Ibn Abbas r.a. Taz. Ibn Kathir) wala sitamwezesha mtu yeyote kukuuwa. Nami nitakunyanyua pahala pa utukufu wangu, na nitakuepusha na maadui wako wanao kusudia kukuuwa, na nitawafanya wanao kufuata wasio kengeuka na dini yako, wawe na nguvu na utawala juu ya wale wasio fuata uwongofu wako, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu ni Akhera. Hapo nitawahukumu katika hayo mlio kuwa mkizozana kwayo katika mambo ya dini.

56 Ama wale wanao kataa kwa ukafiri nitawaonjesha adhabu ya hizaya na mateso kwa kuwasalitisha mataifa mengine juu yao katika dunia, na hakika adhabu ya Akhera ni kali zaidi na ina hizaya zaidi. Na wala hawana wa kuwaokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

57 Na ama walio ongoka kwa uwongofu wa Mwenyezi Mungu, wakatenda vitendo vya kufuata mwendo wa kheri, Mwenyezi Mungu atawapa malipo ya kutosha kwa hizo a'mali zao. Na ndiyo shani yake Mwenyezi Mungu kuwa hawalipi thawabu zake wale wanao pindukia mipaka ya Mwenyezi Mungu wakafanya jeuri ya kutoitikia wito wake na kumtendea wema. Wala hawanyanyulii cheo chao.

58 Hayo tuliyo kusimulia ni miongoni ya hoja zenye kuonyesha ukweli wa ujumbe wako, nayo ni katika Qur'ani Tukufu yenye kukumbusha, na yenye kukusanya ilimu ya manufaa.

kwa udongo kisha akamwambia: Kuwa! Basi akawa.⁵⁹

60. Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanao fanya shaka.⁶⁰

61. Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooi tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.⁶¹

62. Hakika haya ndiyo maelezo ya kweli. Na hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu tu, na hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu na Mwenye hikima.⁶²

63. Na kama wakigeuka basi Mwenyezi Mungu anawajua waharibifu.⁶³

64. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooi kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Waola Walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudi- eni ya kwamba sisi ni Waislamu.⁶⁴

65. Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahim, na hali Taurati na Injili hazikuteremshwa ila baada yake? Basi hamzingatii?⁶⁵

66. Angalieni! Nyinyi mlibishana katika yale mliyo yajua. Mbona sasa mnabishana katika yale msiyo yajua? Na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye, na nyinyi hamjui.⁶⁶

59 Baadhi ya watu wamepotea katika kadhiya ya Isa, wakadai ati kuwa yeye ni Mwana wa Mwenyezi Mungu kwa kuwa kazaliwa bila ya baba. Mwenyezi Mungu anawaambia: Hakika shani ya Isa katika kuumbwa kwake bila ya baba ni kama shani ya Adam alivyo umbwa kwa udongo bila ya baba wala mama. Mwenyezi Mungu alimfanya na akataka awe, akawa mtu sawasawa.

60 Bayana hii katika kuumbwa Isa ndiyo ukweli wenyewe ambao unabainisha hakika yaliyo tokea katika khabari za Mola Mlezi wa viumbe vyote. Basi wewe dumu katika yakini yako wala usiwe katika wenye kutia shaka.

61 Basi wenye kujadiliana nawe, ewe Nabii, katika shani ya Isa baada ya kukujia wewe khabari iliyo toka kwa Mwenyezi Mungu na ambayo haina ubaifu ndani yake, basi waambie kauli itakayo dhihirisha ujuzi wako wa yakini na upotovu wao wa uwongo: Njooi! Kila mmoja wetu na wenu awaite watoto wake, na wakeze na wenyewe nafsi zao. Kisha tumnyenyekee Mwenyezi Mungu kumtaka ateremshe ghadhabu yake na nakama yake juu ya aliye mwongo katika hili jambo la Isa kuzaliwa bila ya baba na kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu wala si Mwana wa Mungu.

62 Hiyo ndiyo kweli isiyo na shaka yoyote. Kwani hapanapo mungu ila Mwenyezi Mungu aliye umbu kila kitu, na Yeye ni pekee katika utukufu wa Ufalme wake na hikima katika uumbaji wake.

63 Wakiikataa Haki baada ya kwisha wadhihirikia, na wasiache upotovu wao, basi hao ndio waharibifu. Na Mwenyezi Mungu anawajua.

64 Sema, ewe Nabii! Enyi Watu wa Kitabu! (Biblia, yaani Mayahudi na Wakristo) njooi kwenye neno moja la uadilifu lenye kutukusanya sote na tunalo litaja, nalo ni kuwa hatumuabudu ila Mwenyezi Mungu tu, wala tusimwekee washirika katika ibada. Na wala tusiwe tunawat'ii baadhi yetu tukiwafuata katika kuhalalisha na kuharimisha, tukaachilia mbali hukumu ya Mwenyezi Mungu katika mambo ya halali na haramu. Wakiukataa wito huu wa haki waambie: Shuhudieni kuwa sisi ni Waislamu, yaani tunafuata hukumu za Mwenyezi Mungu, na Yeye tu tumemsafia Dini, wala hatumwombi mwengineyo. (Taurati:Kutoka 20.3:Usiwe na miungu mingine ila Mimi. Injili ya Marko 12.29 : Yesu akamjibu, [amri] Ya kwanza ndiyo hii, Sikia Israel, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja.)

65 Enyi Watu wa Kitabu! Kwa nini mnazozana na kujadiliana kwa mambo ya Ibrahim, kila mmoja wenu akidai kuwa yeye ndiye anaishika dini yake, na ilhali Ibrahim alikuwako kabla ya Taurati na Injili akifuata sharia mbali. Hizo Taurati na Injili hazikuja ila baadae. Basi atakuwaje yeye afuate sharia za vitabu hivyo? Hamna akili ya kutambua jambo hili lililo wazi?

66 Watu nyinyi mlikuwa mkijadili mambo yalio wakhusu Musa na Isa mnayo yajua kama mnavyo dai wenyewe. Imekuwaje basi hivi sasa kudai kuwa Ibrahim alikuwa Yahudi au Mkristo - jambo ambalo nyinyi hamlijui! Na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kujua hakika ya hayo mnayo gombania, na nyinyi

67. Ibrahim hakuwa Yahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu Muislamu, wala hakuwa katika washirikina.⁶⁷
68. Watu wanao mkaribia zaidi Ibrahim ni wale walio mfuata yeye na Nabii huyu na walio amini. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa Waumini.⁶⁸
69. Kipo kikundi katika Watu wa Kitabu wanao penda kukupotezeni; lakini hawapotezi ila nafsi zao, nao wenyewe hawatambui.⁶⁹
70. Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu ilhali nyinyi mnashuhudia?⁷⁰
71. Enyi Watu wa Kitabu! Mbona kweli mnaivisha uwongo, na kweli mnaificha na hali mnajua?⁷¹
72. Na kikundi katika Watu wa Kitabu walisema: Yaaminini yale waliyo teremshiwa wenye kuamini mwanzo wa mchana, na yakataeni mwisho wake; huenda wakarejea.⁷²
73. Wala msimuamini ila anaye fuata dini yenu. Sema: Hakika uwongofu ni uwongofu wa Mwenyezi Mungu, kuwa apewe mtu mfano wa mlio pewa nyinyi au wakuhojini mbele ya Mola wenu Mlezi. Sema: Hakika fadhila zimo mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mjuzi.⁷³
74. Yeye humchagua kumpa rehema zake amtakaye; na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye fadhila kubwa.⁷⁴
75. Na miongoni mwa Watu wa Kitabu yupo ambaye ukimpa amana ya mrundi wa

hamjui kitu.

67 Hakika Ibrahim a.s. hakufuata dini ya Kiyahudi wala dini ya Kikristo, lakini ameachana na dini zote za upotovu na akashika Dini ya Haki, ya Uislamu, yaani kumwelekea Mwenyezi Mungu, na kumtakasia Yeye kwa ut'iifu, na wala hakuwa miongoni wa hao wanao mshirikisha Mwenyezi Mungu katika kuabudu.

68 Hakika wenye haki kabisa kunasibiana na Ibrahim na Dini yake ni wale walio mwikia wito wake na wakaongoka kufuata uwongofu wake katika zama zake, na vile vile Muhammad s.a.w. na walioamini pamoja naye. Kwani hao ni watu wa Tawhidi safi ya kweli, kumwamini Mwenyezi Mungu mmoja bila ya walakini. Hiyo ndiyo Dini ya Ibrahim. Mwenyezi Mungu anawapenda Waumini, na Yeye atawanusuru, kwani wao ni vipenzi vyake, na atawalipa kwa mema na ziada.

69 Kipo kikundi katika Watu wa Kitabu wanao tamani kuwapotoa Waumini na kuwafitini waache Dini yao, kwa kuwatilia mikorogo ya kudhoofisha itikadi. Lakini katika kazi yao hii hawatampotoa mtu ila nafsi zao wenyewe kwa kuendelea katika upotovu, ambao utakuja kuwagubika wao wenyewe tu, na wala hawajui kuwa matokeo ya juhudi yao ovu yatawapata wenyewe, wala hayatawadhuru Waumini.

70 Enyi Watu wa Kitabu! Kwa nini mnakanusha Aya na Ishara za Mwenyezi Mungu zilizo teremka kuthibitisha Unabii wa Muhammad, s.a.w. na hali nyinyi mnajua haki?

71 Enyi Watu wa Kitabu! Kwa nini mkachukua Haki waliyo kuja nayo Manabii, na ikateremshiwa Vitabu, mkaichanganya na mambo ya udanganyifu ya kubuni na mkaleta tafsiri potovu, na msieneze Haki safi iliyo wazi isiyo kuwa na mchanganyiko? Na nyinyi mwajua vyema kuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kitendo kama hichi ni kubwa.

72 Katika mtindo wao wa kutaka kuwapotoa Waumini, hawa Watu wa Kitabu wakiwaambia wenzao: Jitieni kuiamini Qur'ani aliyote teremshiwa Muhammad asubuhi, na ikifika jioni ikataeni. Huenda kwa hivyo mkawafitini hawa kwa kuwaingiza shaka katika nyoyo zao, wakaiacha dini yao.

73 Aidha wao husema: Msiwakubalie ila aliyote fuata dini yenu, asije yeyote kati yao akadai kuwa nao wamepewa kama mlio pewa nyinyi, au akachukulia hoja mbele ya Mola wenu Mlezi kwa kuwakubalia kwenu. Ewe Nabii! Waambie: Hakika uwongofu wote unateremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye anaye mmiminia na kumteua amtakaye. Na ewe Nabii! Waambie: Hakika fadhila ziko kwa Mwenyezi Mungu humpa amtakaye katika waja wake, na Yeye ni Mkunjufu wa fadhila, Mjuzi wa anaye stahiki hayo na anaye teremkiwa na hayo.

74 Yeye Mwenyezi Mungu humpa amtakaye Unabii na Utume, na anaye mkhusisha kwa kumpa hayo ni katika fadhila yake tu. Na Mwenyezi Mungu ana fadhila kubwa kubwa kabisa, na wala hapana anaye muingilia yeyote, wala hapana anaye mzuia katika kutoa kwake.

mali atakurudishia, na miongoni mwao yupo ambaye ukimpa amana ya dinari moja hakurudishii isipo kuwa ukimsimamia kum dai. Haya ni kwa kuwa wakisema: Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasio jua kusoma. Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua.⁷⁵

76. Sivyo hivyo, bali anaye timiza ahadi yake na akamchamngu basi Mwenyezi Mungu huwapenda wachamngu.⁷⁶

77. Hakika wanao uza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao thamani ndogo, hao hawatakuwa na sehemu ya kheri yoyote katika Akhera, wala Mwenyezi Mungu hatasema nao wala hatawatazama Siku ya Kiyama, wala hatawatakasaa, nao watapata adhabu chungu.⁷⁷

78. Na wapo baadhi yao wanao pindua ndimi zao katika kusoma Kitabu ili mdhanie kuwa hayo yanatoka Kitabuni, na wala hayatoki Kitabuni. Na husema: Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu. Na wala hayatoki kwa Mwenyezi Mungu. Na wanamsingizia Mwenyezi Mungu uwongo na wao wanajua.⁷⁸

79. Haiwezi kuwa mtu aliye pewa na Mwenyezi Mungu Kitabu na hikima na Unabii kisha awaambie watu: Kuweni wa kuniabudu mimi badala ya Mwenyezi Mungu. Bali atawaambia: Kuweni wenye kumuabudu Mola Mlezi wa viumbe vyote, kwa kuwa nyinyi mnafundisha Kitabu na kwa kuwa mnakisoma.⁷⁹

80. Wala hatakuamrisheni kuwafanya Malaika na Manabii kuwa ni miungu. Je, atakuamrisheni ukafiri baada ya kuwa nyinyi Waislamu?⁸⁰

75 Huo ndio mwendo wao Watu wa Biblia katika itikadi, ama mwendo wao katika mambo ya mali utaona: Kati yao kuna ambaye ukimpa amana ya chungu ya dhahabu au fedha atakurejeshea sawa sawa bila ya kupunguka chochote. Na mwengine kati yao ukimpa amana ya dinari moja tu hakurudishii, ila ikiwa utamshikilia mpaka aitoe. Haya ni kwa sababu wapo baadhi yao wanawaona watu wa mataifa mengine, si watu wa Biblia basi haiwalazimu wao kuwatendea haki, na wanadai kuwa hiyo ni hukumu ya Mwenyezi Mungu. Na wao wanajua vyema kuwa hayo ni kumzulia uwongo Mwenyezi Mungu. (Tazama katika Agano la Kale: Kumbukumbu la Torati, 23.19-20 inaruhusu kumnyonya riba mtu mbali asiyekuwa Yahudi. Kumbukumbu 12.21 inaruhusu kumlisha nyamafu mgeni na kumuuzia pia. Uzushi kama huu unakashifiwa na Aya 78 ifuatayo kuwa haya hayakutokana na Mwenyezi Mungu, bali wamepachika wao tu katika vitabu vyao.)

76 Hakika ni kweli wamemzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Kwani mwenye kumrejeshea mwenyewe haki yake na akamtimiza kwa wakati wake kama alivyo ahidi, na akamwogopa Mwenyezi Mungu, wala asipunguze kitu wala asiakhirishe, huyo basi atapata mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwa sababu amemcha Yeye.

77 Wanao iacha ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyo fungamana nao ya kuwa watazitimiza haki na watasimamia yaliyo waajibu, wala hawatoacha viapo vyao walivyo apa kuwa watatimiza - kwa thamani ndogo ya faida ya dunia, na ingawa kuu katika maoni yao, hao hawatakuwa na sehemu yoyote katika raha za Akhera. Mola wao Mlezi atawapuuza, wala hatowaangalia kwa jicho la rehema Siku ya Kiyama, wala hatowafutia dhambi zao, na watapata adhabu chungu ya kuendelea.

78 Katika Watu wa Kitabu wapo ambao huzipindua ndimi zao kutamka maneno yasiyo kuwamo katika Kitabu kwa lafdhi ya Kitabu, watu wadhania kuwa ni maneno yanayo toka kwa Mwenyezi Mungu, na wala hayamo katika ufunuo wa Mwenyezi Mungu. Wanamzulia Mwenyezi Mungu nao ndani ya nafsi zao wanajua kuwa wanasema uwongo.

79 Si akili wala haimfalii mwanaadamu aliye teremshiwa Kitabu na Mwenyezi Mungu na akapewa ilimu ya manufaa na kuweza kuzungumza mambo yanayo tokana na Mwenyezi Mungu, tena awatake watu wamuabudu yeye badala ya kumuabudu Mwenyezi Mungu. Lakini linalo ingia akilini, na lifaalo, ni kuwa yeye awatake watu wamsafie ibada Mola wao Mlezi aliye waumba kwa mujibu alivyo wafunza kutokana na ilimu ya Kitabu na kwa mujibu ya wanayo soma.

80 Wala hayumkini akuamrisheni kuwafanya Malaika au Manabii kuwa ndio miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Ni ukafiri usio ingia akilini kukuamrisheni hayo baada ya kuwa mmekwisha kuwa Waislamu

81. Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia.⁸¹

82. Watakao geuka baada ya haya basi hao ndio wapotovu.⁸²

83. Je, wanataka dini isiyo kuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumt'ii Yeye kikipenda kisipende, na kwake Yeye watarejeshwa?⁸³

84. Sema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu, na tuliyo teremshiwa sisi, na aliyo teremshiwa Ibrahim, na Ismail, na Is-haak na Yaakub na wajukuu zao, na aliyo pewa Musa na Isa na Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi. Hatubagui baina yao hata mmoja, na sisi ni wenye kusilimu kwake.⁸⁴

85. Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri.⁸⁵

86. Mwenyezi Mungu atawaongoaje watu walio kufuru baada ya kuamini kwao, na wakashuhudia ya kuwa Mtume huyu ni wa haki, na zikawafikia hoja zilizo wazi? Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.⁸⁶

87. Hao malipo yao ni kuwa ipo juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote.⁸⁷

mlio muelekezea nyuso Mwenyezi Mungu. (Nabii Isa a.s. hakujidaia Ungu hata katika Injili hizi zilizo korogwa, wala hakumfanya Roho Mtakatifu, ambaye ni Malaika, kuwa ni Mungu.)

81 Ewe Nabii! Watajie kuwa Mwenyezi Mungu aliahidiana na akaagana na kila Nabii aliye teremshiwa Kitabu na akapewa ilimu ya manufaa, ya kwamba akija Mtume ambaye wito wake unakubaliana na wito wao basi ni waajibu wao wamuamini na wamsaidie. Na Manabii wote walikiri kuitimiza ahadi hiyo, na wakakiri na wakashuhudia kwa nafsi zao, na Mwenyezi Mungu akawashuhudia hayo. Tena wao wakayafikisha hayo kwa kaumu zao. Ahadi hiyo imewapasia wao imani na wamnusuru wakimwahi. Kama hawakumwahi basi ni waajibu wa kaumu zao wamuamini na wamnusuru kwa kutimiza na kufuata yaliyo walazimu Manabii wao. (Tazama katika Biblia: Kumbukumbu 18.17-19, Injili ya Yohana 16.7-14)

82 Anaye kataa kumuamini Nabii huyu baada ya ahadi hii madhubuti ni mpotovu aliye toka kwenye sharia ya Mwenyezi Mungu, ni kafiri mwenye kuwakataa Manabii wote wa mwanzo mpaka wa mwisho.

83 Je, wanataka dini isiyo kuwa Dini ya Muhammad, na hiyo ndiyo Dini ya Manabii wote? Dini hii ndiyo pekee Dini ya Mwenyezi Mungu anaye nyenyekewa na kila kilichomo mbinguni na duniani kwa ut'iifu, kwa kupenda na khiasi, au kwa lazima kwa kufuata tabia na maumbile. Na kwake Yeye ndio viumbe vyote vinarejea.

84 Mwenyezi Mungu ametilia mkazo kuwa Yeye ni Mmoja, na Ujumbe wake ni mmoja. Amemuamrisha Nabii wake na walio pamoja naye wasema: Tumesadiki kuwa Mwenyezi Mungu ndiye peke yake anaye faa kuabudiwa, na ndiye anaye watuma Mitume wake. Na tumeiamini Qur'ani na Sharia aliyo tuteremshia Mwenyezi Mungu, na pia tumeamini Vitabu na Sharia alizo wateremshia Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yaakub na watoto wao thinaashara, na aliyo teremsha Mwenyezi Mungu kwa Musa, nayo ni Taurati, na kwa Isa, nayo ni Injili, na walio teremshiwa Manabii wote walio baki. Hapana khitilafu katika kuamini baina ya yeyote katika wao. Na sisi kwa hivyo tumeuelekeza uso wetu kwa Mwenyezi Mungu.

85 Baada ya kupata utume Muhammad s.a.w. akitaka mtu dini na sharia zisio kuwa Dini ya Islamu na Sharia yake, Mwenyezi Mungu hatamkubalia. Na malipo ya mtu huyo Siku ya Malipo ni kuwa miongoni mwa walio zikhasiri nafsi zao, ikawajibikia adhabu chungu.

86 Mwenyezi Mungu hakubaliani na watu walio kwisha shuhudia kuwa Mtume ni wa haki, na zikawajia dalili za kuonyesha hayo, kisha baada ya yote hayo wakamkataa, na wakakataa miujiza yake. Huo basi ni udhaalimu wao, na Mwenyezi Mungu hakubaliani na madhaalimu.

87 Adhabu ya watu hao wataipata kutoka kwa Mwenyezi Mungu kama wanavyo stahiki kukasirika kwake juu yao, na laana yake, na laana ya bora ya viumbe vyake miongoni mwa Malaika na wanaadamu.

88. Humo watadumu. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa nafasi.⁸⁸
89. Isipo kuwa wale walio tubu baada ya hayo na wakatengenea; kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.⁸⁹
90. Hakika wale walio kufuru baada ya kuamini kwao, kisha wakazidi kukufuru, toba yao haitakubaliwa, na hao ndio walio potea.⁹⁰
91. Hakika wale walio kufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangelitoa. Hao watapata adhabu chungu, wala hawatakuwa na wa kuwanusuru.⁹¹
92. KABISA HAMTAFIKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua.⁹²
93. Kila chakula kilikuwa halali kwa Wana wa Israili isipo kuwa alichojizulia Israili mwenyewe kabla haijateremshwa Taurati. Sema: Leteni Taurati muisome ikiwa nyinyi ni wasema kweli.⁹³
94. Na wanao mzulia uwongo Mwenyezi Mungu baada ya hayo, basi hao ndio madhaalimu.⁹⁴
95. Sema: Mwenyezi Mungu amesema kweli. Basi fuateni mila ya Ibrahim mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.⁹⁵
96. Hakika Nyumba ya kwanza walio wekewa watu kwa ibada ni ile iliyoko Bakka, iliyo barikiwa na yenye uwongofu kwa walimwengu wote.⁹⁶

88 Laana hiyo haitowabanduka, wala hawatapunguziwa adhabu, wala hawapewi muhula.

89 Lakini wale ambao wamejing'oa na madhambi yao, wakaingia kati ya watu wema, wakayaondoa waliyo yahari, basi hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu atawafutia madhambi yao, kwani maghfira na rehema ni miongoni mwa sifa za dharti yake Tukufu.

90 Kukubaliwa toba na kupata rehema ya maghfira kunashurutishwa mtu adumu juu ya Imani. Wanao ipinga Haki baada ya ut'iifu na kusadiki, na wakazidisha upinzani na ufisadi na kuwaudhi Waumini, Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* hatokubali toba yao. Haiwezi kuwa toba yao hiyo ni kweli na safi na hali wanaendelea na vitendo vyao, wapo mbali na Haki na wanaigeuzia nyuso zao.

91 Wale wanao ipinga Haki wala hawafuati, na wanaendelea na uwovu wao mpaka wakafa nao ni wapinzani tu, basi yeyote miongoni mwao hawezi kujitolea fidia ya kujiepusha na adhabu ya Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la*, hata ikawa anacho kitoa kuwa fidia ni dhahabu ya kujaza dunia nzima kama angeweza. Na adhabu yao ina uchungu mkali.

92 Enyi Waumini! Hamtoipata kheri kaamili mnayo itaka na itakayo mridhisha Mwenyezi Mungu ila mkitoa katika vitu mnavyo vipenda na mkatoa katika *Sabili Llahi*, Njia ya Mwenyezi Mungu, kwa namna mbali mbali. Na chochote mnacho kitoa, kidogo na kikubwa, kilio bora au chenginecho, Mwenyezi Mungu anakijua. Kwani Yeye ni Mwenye Kujua, hapana kitu kilioko mbinguni au duniani kinacho fichikana naye.

93 Mayahudi waliwatoa kombo Waislamu kwa kuhlalisha baadhi ya vyakula kama nyama ya ngamia na maziwa yake. Wakadai kuwa hayo yaliharimishwa na sharia ya Ibrahim. Mwenyezi Mungu *Subhanahu* aliwarudi madai yao hayo kwa kubainisha kuwa vyakula vyote vilikuwa halali kwa Wana wa Yaakub (ndiye Israil) kabla ya kuteremka Taurati, ila alichojizua Yaakub mwenyewe kwa sababu zilizo mkhusu yeye tu, basi na wao wakijiharimishia nafsi zao. Mwenyezi Mungu akamuamrisha Nabii wake awatake walete uthibitisho wa Taurati kuwa sharia ya Ibrahim imeharimisha hayo kama wao wanasema kweli. Wakashindwa, wakanywea.

94 Ilipo thibiti kuwa wameemewa basi wenye kumsingizia uwongo Mwenyezi Mungu baada ya hoja hizo, hao ndio walio selevela na udhaalimu wao, na wanastahiki kuitwa Madhaalimu.

95 Baada ya kushindwa kwao Mwenyezi Mungu amemuamrisha Nabii wake awabainishie kuwa ukweli wa Mwenyezi Mungu umethibiti katika ayasemayo. Basi ifuateni Sharia ya Ibrahim anayo kutakeni muifuate, na nyinyi mnaikanusha. Hii ni mbali kabisa na hizo dini za uwongo, kwani Ibrahim hakuwa miongoni mwa washirikina.

96 Katika kufuata mila ya Ibrahim ni kuelekea wakati wa Sala Nyumba aliyo ijenga, na kwenda kuhiji

97. Ndani yake zipo Ishara zilizo wazi - masimamio ya Ibrahim, na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani. Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakaye kanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu.⁹⁷

98. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Kwa nini mnakanusha ishara za Mwenyezi Mungu, na ilhali kuwa Mwenyezi Mungu ni Shahidi kwa yote mnayo yatenda?⁹⁸

99. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Kwa nini mnamzuilia aliye amini Njia ya Mwenyezi Mungu mkiitafutia kosa, na hali nyinyi mnashuhudia? Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na mnayo yatenda.⁹⁹

100. Enyi mlio amini! Mkiwat'ii baadhi ya walio pewa Kitabu watakurudisheni kuwa makafiri baada ya Imani yenu.¹⁰⁰

101. Na vipi mkufuru hali nyinyi mnasomewa Aya za Mwenyezi Mungu na Mtume yuko kati yenu? Na mwenye kushikamana na Mwenyezi Mungu basi huyo ameongozwa kwenye Njia Iliyo Nyooka.¹⁰¹

102. Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu.¹⁰²

103. Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile mlivyo kuwa nyinyi kwa nyinyi maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto, naye akakuokoeni nalo.

huko. Mwenyezi Mungu amebainisha hayo kwa kusema: Hakika Nyumba ya awali kwa ukongwe na utukufu aliyo ijaalia Mwenyezi Mungu iwe ni ya ibada kwa watu ni hiyo iliyoko Makka (au Bakka kama pia inavyoitwa). Nayo ina kheri nyingi na manufaa, na Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* ameijaalia iwe na baraka. Nayo Nyumba hiyo ni pahali pa uwongofu kwa watu kwa kuhiji na kuelekea wakati wa Sala.

97 Zipo dalili wazi za kuonyesha utakatifu wake huo Msikiti wa Makka na kuzidi fadhila zake. Miongoni mwa hizo ni hapo alipo kuwa akisimama Nabii Ibrahim a.s. kwa kusali. Na pia kuwa anaye ingia humo huwa amesalimika halimpatu ovu. Na kuhiji Makka ni waajibu wa kila mtu awezae kwenda. Na mwenye kukataa, akaiasi amri ya Mwenyezi Mungu, na akaipinga Dini yake, basi khasara itamuangukia mwenyewe, na Mwenyezi Mungu anajitosha, hawahitajii watu wote.

98 Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* amemuamrisha Mtume wake awahizi Watu wa Kitabu kwa kuendelea kwao kukufuru na kupotoka na kupotosha, akasema: Enyi Watu wa Kitabu! Huo ukafiri wenu hauna Sura wala maana. Kwa sababu gani mnakanusha dalili, na hoja za Mwenyezi Mungu zenye kuthibitisha Unabii na Ukweli wa Muhammad? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuvijua vitendo vyenu na atakulipeni malipo yake.

99 Enyi Watu wa Kitabu! Vipi mnajaribu kumgeuza mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kuifuata Haki aache Njia Iliyo Nyooka ya Mwenyezi Mungu wa Kweli, na mnajaribu kuikosoa Njia hiyo, na nyinyi mnajua kuwa hiyo ndiyo Haki? Wala Mwenyezi Mungu hakughafilika na vitendo vyenu, naye atakulipeni kwavyo.

100 Mwenyezi Mungu anawahadharisha Waumini na vitimbi vya baadhi ya Watu wa Kitabu, (Mayahudi na Wakristo), vya uchochezi wao wa udanganyifu kwa kusema: Mkiwat'ii baadhi ya Watu wa Kitabu katika yale wanayo yaeneza ya kutilisha shaka katika Dini yenu, itakuwa mnarajea tena kwenye upotovu baada ya uwongofu, na wakurejezeni muwe makafiri baada ya kuwa ni Waumini.

101 Hebu izangitieni hali yenu ya ajabu, kuwa mnapotoka na mnakufuru baada ya Imani, na hali mnasomewa Qur'ani, na Mtume mnaye, anakubainishieni na anakuingeni na upotovu katika Dini yenu. Na mwenye kumkimbilia Mola wake Mlezi, na akashikamana na Dini yake, basi huyo amefanya vyema. Mola wake Mlezi amemwongoa kwenye Njia ya kufuzu na kufaulu.

102 Hakika mlango wa shari uwazi ikiwa hamumchi Mwenyezi Mungu. Basi enyi mlio amini! Mkhofuni Mwenyezi Mungu kwa khofu inayopasa, kwa kutenda anayo amrisha, na kuyaepuka anayo yakataza. Na dumuni juu ya Uislamu mpaka mtakapo kutana na Mwenyezi Mungu.

Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Ishara zake ili mpate kuongoka.¹⁰³

104. Na uwe kutokana na nyinyi umma unao lingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio walio fanikiwa.¹⁰⁴

105. Wala msiwe kama wale walio farikiana na kukhitalifiana baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi. Na hao ndio watakao kuwa na adhabu kubwa.¹⁰⁵

106. Siku ambayo nyuso zitanawiri na nyuso zitasawijika. Ama hao ambao nyuso zao zitasawijika wataambiwa: Je! Mlikufuru baada ya kuamini kwenu? Basi onjeni adhabu kwa vile mlivyo kuwa mnakufuru.¹⁰⁶

107. Ama wale ambao nyuso zao zitanawiri watakuwa katika rehema ya Mwenyezi Mungu. Wao humo wataadumu.¹⁰⁷

108. Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu tunakusomea kwa haki. Na Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu walimwengu.¹⁰⁸

109. Na kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini ni cha Mwenyezi Mungu; na mambo yote yatarejea kwa Mwenyezi Mungu.¹⁰⁹

110. Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa Watu wa Kitabu nao wameamini ingeli kuwa bora kwao. Wapo miongoni mwao waumini, lakini wengi wao wapotovu.¹¹⁰

111. Maadui hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni

103 Nyote nyinyi shikamaneni na Dini ya Mwenyezi Mungu, wala msifanye jambo litalo leta mfarakano baina yenu. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu mlivyo kuwa wakati wa ujahili nyinyi kwa nyinyi maadui. Mwenyezi Mungu akaziunganisha nyoyo zenu kwa Uislamu, mkawa mnapendana, na ilhali kwa sababu ya ukafiri wenu na kufarikiana kweni mlikuwa juu ya ukingo wa Moto, akakuokoeni kwa Uislamu. Kwa mfano wa bayana kama hii ya pekee Mwenyezi Mungu anakubainishieni daima njia za kheri, ili mdumu katika uwongofu.

104 Hakika njia ya kuungana kuliko kamilika juu ya Haki katika kivuli cha Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kivuli cha Mtume wake, ni kuwa muwe nyinyi Umma unao lingania (unao itia) watu waje wafuate mwendo utao waletea maslaha ya Dini na dunia, uamrishe ut'iifu kwa Mwenyezi Mungu, ukataze maasia. Na hapo ndipo mtakuwa mlio fuzu, kufuzu kulio kamilika.

105 Wala msiwe kwa kupuuza kwenu kuamrisha mema na kukataza maovu--mambo ambayo ndiyo yanayo kukusanyeni katika kheri na Dini ya Haki--kama wale walio puuza kuamrisha mema na kukataza maovu, wakagawika mapande mbali mbali, wakakhitalifiana katika dini yao baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, zenye kubainisha Haki. Na hao walio farikiana wakakhitalifiana, watapata adhabu kuu.

106 Adhabu kuu hiyo itakuwa Siku zitapo nawiri nyuso za Waumini kwa furaha, na kusawijika kwa masikitiko na huzuni nyuso za makafiri. Wataambiwa kwa kuwatahayarisha: Je, mmekufuru baada ya kuwa mlulikulia juu ya Imani na ut'iifu wa haki, na mkaletewa hoja zilizo wazi? Basi onjeni adhabu kwa sababu ya ukafiri wenu!

107 Ama wale nyuso zao zimekuwa nyeupe, yaani zimenawiri, kwa kufurahi, hao watakuwa katika Pepo ambayo Mwenyezi Mungu amewapa kwa rehema yake, wadumu humo milele.

108 Na hizo Aya zilizo kuja za kueleza kuwa mwema na mwovu watalipwa tunakusomea, nazo zimekusanya haki na uadilifu. Na Mwenyezi Mungu hataki kumdhulumu yeyote kati ya watu na majini. 109 Na vyote vililomo mbinguni na ardhini ni vya Mwenyezi Mungu peke yake, ni vyake kwa kuvumba, na kuvimiliki, na kuvisarifu. Na marejeo ya mambo yao ni kwake Yeye. Kwa hivyo humlipa kila mmoja kama anavyo stahiki.

110 Nyinyi Umma wa Muhammad ni bora ya umati alio umbwa Mwenyezi Mungu kwa manufaa ya watu, maadamu mtaamrisha ut'iifu na mtakataza maasi, na mtakuwa ni wenye kumuamini Mwenyezi Mungu kwa Imani safi na ya kweli. Na lau kuwa Watu wa Kitabu wangu kuwa ni wakweli katika imani yao kama nyinyi, basi ingeli kuwa ni bora kwao kuliko walivyo. Walakini baadhi yao ni Waumini, na wengi wao wamekiuka mipaka ya Imani na yanayo pasa.

mgongo, na tena hawatanusuriwa.¹¹¹

112. Wamepigwa na udhalili popote wanapo kutikana, isipo kuwa wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu. Na wakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na wamepigwa na unyonge. Hayo ni kwa sababu walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakiwauwa Manabii pasina haki; hayo ni kwa sababu waliasi na walikuwa wakiruka mipaka.¹¹²

113. Wote hao si sawa sawa. Miongoni mwa Watu wa Kitabu wamo watu walio simama baraabara, wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku, na pia wanasujudu.¹¹³

114. Wanamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wanaamrisha mema na wanakataza maovu na wanakimbilia katika mambo ya kheri. Na hao ndio miongoni mwa watenda mema.¹¹⁴

115. Na kheri yoyote wanayo ifanya hawatanyimwa malipwa yake. Na Mwenyezi Mungu anawajua wachamngu.¹¹⁵

116. Hakika wale walio kufuru hazitawafaa kitu mali zao wala watoto wao mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio watu wa Motoni - humo watadumu.¹¹⁶

117. Mfano wa vile wanavyo vitoa katika uhai wao wa duniani ni kama upepo ambao ndani yake ipo baridi ya barafu, ukalisibu shamba la watu walio dhulumu nafsi zao, ukaliteketeza. Na Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu, bali wao wenyewe wanadhulumu nafsi zao.¹¹⁷

118. Enyi mlio amini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasio kuwa katika nyinyi. Hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yanayo kudhuruni. Imekwisha

111 Hao wapotovu hawawezi kukudhuruni nyinyi kama walivyo kuandalieni, wala hawakuathirini. Ijapo kuwa mtapata maudhi kwao, lakini athari yake haiselelei. Na hata wakipigana nanyi wataingia kiwewe wakimbie wasipambane nanyi, na hapo mwisho hawatopata ushindi juu yenu maadamu nyinyi mtashikamana na kuamrisha mema na kukataza maovu.

112 Na Mwenyewe Subhana ameeleza kuwa lazima watapata madhila popote watapo kutikana, ila wakifungamana kwa ahadi ya Mwenyezi Mungu na ahadi ya Waislamu. Na wao wamestahiki wapate ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na pia Mwenyezi Mungu amewajaalia lazima uwafikie unyonge na unyenyekevu kwa wengineo. Na hayo ni kwa sababu ya kukataa kwao Ishara zote za Mwenyezi Mungu zinazo onyesha Unabii wa Muhammad s.a.w. na vile kuridhi kwao hapo zamani kuuliwa Manabii ambako hakuwezi kuwa ni kwa haki, bali ni kwa uasi wao na uadui wao.

113 Watu wa Kitabu si wote sawa sawa. Miongoni mwao wapo walio simama msimamo mwema, wa uadilifu, wanakisoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu nyakati za usiku wakisali.

114 Wanaamini kweli kuwepo Mwenyezi Mungu, na kuwa Yeye ni Mmoja tu. Wanaamini Mitume wote, hawamuabudu ila Mwenyezi Mungu. Na wanaamini kuwa itafika Siku ya Kiyama; wanaamrisha ut'ifu kwa Mwenyezi Mungu, na wanakataza maasi, na wanawania kutenda mambo ya kheri. Hawa kwa Mwenyezi Mungu huhisabiwa miongoni mwa watenda wema.

115 Kheri yoyote wanayo ifanya watu hao hawatonyimwa thawabu zake. Na Mwenyezi Mungu amezitunguka kwa kuzijua na kuziweza hali zao na malipo yao.

116 Wale walio kufuru, mali yao na wangayatoa kuwa ni fidia hayatowafaa kitu, wala watoto wao na wangawataka msaada hawatoweza kuwasaidia hata chembe kuwakinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu katika Akhera. Na hawa ndio walio lazimika kuingia Motoni na waselelee humo.

117 Hakika hali ya wanacho kitoa makafiri duniani kuwa ni sadaka au cha kuwakaribisha mbele ya Mwenyezi Mungu Akhera mfano wake, kwa kuwa ni kazi bure katika ujira wa vitendo, ni kama hali ya shamba la watu walio jidhulumu nafsi zao kwa ukafiri na maasi. Shamba hilo likakumbwa na upepo wenye baridi kali ya barafu, likateketea shamba lote kuwa ni malipo yao. Wala Mwenyezi Mungu siye aliye wadhulumu ujira wa kazi yao, lakini ni wao wenyewe ndio walio jidhulumu nafsi zao kwa kufanya yaliyo sabibisha hayo. Nayo ni kuzipinga dalili na ushahidi wa Imani na kumkufuru Mwenyezi Mungu.

fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayo ficha vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekwisha kubainishieni Ishara ikiwa nyinyi mtayatia akilini.¹¹⁸

119. Hivyo basi nyinyi ndio mnawapenda watu hao, wala wao hawakupendeni. Nanyi mnaviamini Vitabu vyote. Na wanapo kutana nanyi husema: Tumeamini. Na wanapo kuwa peke yao wanakuumieni vidole kwa chuki. Sema: Kufeni kwa chuki yenu! Hakika Mwenyezi Mungu anayajua yaliomo vifuani.¹¹⁹

120. Ikikupateni kheri huwaudhi. Na ikikupateni shari wanafurahia. Na nyinyi mkisubiri na mkajizuilia, hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyazunguka yote wayatendayo.¹²⁰

121. Na pale ulipo toka asubuhi, ukaacha ahali zako uwapange Waumini kwenye vituo kwa ajili ya vita - na Mwenyezi Mungu anasikia na anajua.¹²¹

122. Makundi mawili miongoni mwenu yakaingiwa na woga kuwa watashindwa - na hali Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wao; na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.¹²²

123. Na Mwenyezi Mungu alikwisha kunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge. Basi mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kushukuru.¹²³

124. Ulipo waambia Waumini: Je, haitakutosheni ikiwa Mola wenu atakusaidieni kwa Malaika elfu tatu walio teremshwa?¹²⁴

125. Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamngu na hata maadui wakikutokeeni

118 Enyi mlio amini! Msitafute kuwafanya marafiki wa ndani watu wasio wa Dini yenu mkatumai msaada kwao, na mkawa mkiwapa siri zenu. Hao hawatoacha kuyafisidi mambo yenu, kwani wao wanapenda mno kukutieni taabuni na kukudhuruni kwa madhara makubwa. Zimekwisha dhiri ishara za bughdha yao kukuchukieni nyinyi katika kuropokwa ndimi zao. Na yaliyo ficha nyoyo zao ni makubwa zaidi. Tumekwisha kuonyesheni alama za kumtambua rafiki na adui kama nyinyi ni watu wa akili na utambuzi wa kweli.

119 Enyi nyinyi Waumini! Mnawapenda hawa makafiri na wanaafiki kwa ajili ya ujamaa, au urafiki au mapenzi tu. Na wao, lakini, hawakupendeni kwa sababu ya kuing'ang'anilia dini yao. Na nyinyi mnaamini Vitabu vyote vilivyo teremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wanapo kutana nanyi hujitia imani ili kukudanganyeni. Na wakisha kuacheni huziuma ncha za vidole vyao kwa chuki na kukasirika. Ewe Nabii! Waambie: Endeleeni na hiyo chuki yenu mpaka mfe! Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyajua yanayo fichikana vifuani, na atakulipeni kwavyo.

120 Nyinyi mkipata neema, kama vile kushinda vitani na ngawira, wao husikitika. Mkipata msiba kama ukame na kushindwa, wao hufurahia msiba wenu. Lakini nyinyi mkisubiri juu ya maudhi yao, na mkajizuilia na kule kuwafanya urafiki mliko katazwa, basi maudhi yao na uadui wao hautakudhuruni kitu. Kwani Yeye Aliye tukuka anavijua vyema vitimbi wanavyo vifanya, wala Yeye hashindwi kukulindeni nao.

121 Na hebu taja Ewe Nabii! Pale ulipo toka asubuhi mapema ukaacha ahali zako, watu wako wa nyumbani, ukenda mpaka Uhud kwa makusudi ya kuwaweka Waumini katika makao yao kwa ajili ya vita. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia kauli zenu, ni Mwenye kuzijua niya zenu.

122 Ilipo tokea kuwa vikundi viwili vya Waumini kuingiwa na khofu ya kushindwa na wakataka kurejea nyuma, Mwenyezi Mungu aliwalinda akawapa moyo wa kuthibiti, wakasonga mbele katika vita. Kwani hakika Mwenyezi Mungu ndiye mwenye utawala katika mambo yao mawili, na ndiye wa kuwalinda na kuwawezesha kwa kuwapa tawfiqi. Basi Waumini nawachukue funzo kutokana na haya, na wamtegemee Yeye ili awanusuru.

123 Mwenyezi Mungu amewakumbusha Waumini ile neema ya nusura aliyo wapa katika vita vya Badri waliposubiri. Akawahakikishia kuwa Yeye ndiye aliye wapa ushindi katika vita vile na ingawa walikuwa wachache na wapungufu wa silaha; akawataka wamt'ii kuwa ni shukrani kwa neema hiyo. (*Tazama Maelezo 3:123*)

124 Ushindi ulipatikana Mtume alipo waambia Waumini: Haitatosha kukutulizeni nafsi zenu Mola wenu Mlezi akikusaidieni kwa Malaika elfu tatu watakao letwa ili kukutieni nguvu?

kwa ghafla, basi hapo Mola wenu Mlezi atakusaidieni kwa Malaika elfu tano wanao shambulia kwa nguvu.¹²⁵

126. Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na ili nyoyo zenu zipate kutua. Na msaada hautoki isipo kuwa kwa Mwenyezi Mungu, Aliye tukuka, Mwenye nguvu na Mwenye hikima.¹²⁶

127. Haya ni kwa ajili awakate sehemu katika walio kufuru, au awahizi wapate kurejea nyuma nao wamepwelewa.¹²⁷

128. Wewe huna lako jambo katika haya - ama atawahurumia au atawaadhibu, kwani wao ni madhaalimu.¹²⁸

129. Na ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi. Yeye humsamehe na humuadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mwenye kurehemu.¹²⁹

130. Enyi mlio amini! Msile riba mkizidisha juu kwa juu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.¹³⁰

131. Na uogopeni Moto ambao umeandaliwa kwa ajili ya makafiri.¹³¹

132. Na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa.¹³²

133. Na yakimbilieni maghfira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyo wekwa tayari kwa wachamngu,¹³³

134. Ambao hutoa wanapo kuwa na wasaa na wanapo kuwa na dhiki, na wanajizua ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema;¹³⁴

125 Ndio! Msaada huo unakutosheni. Na pindi mkivumilia vita, na mkashikilia uchamngu, na hata maadui zenu wakikutokeeni kwa ghafla, Mola wenu Mlezi atawaongeza hao Malaika mpaka wafike elfu tano ili kukupeni nguvu.

126 Na wala Mwenyezi Mungu hakujaalia huko kukuleteeni msaada wa Malaika ila iwe ni bishara tu kwenu ya ushindi, na zipate kutulia nyoyo zenu. Na hapana ushindi ila unao tokana na Mwenyezi Mungu Mwenye Kushinda wote, ambaye anapanga kila kitu kwa pahala pake, na anaye wapangia mambo waja wake Waumini.

127 Naye Mwenyezi Mungu amekupeni ushindi ili watekete baadhi ya wale walio kufuru kwa kuuwawa, au wadhhalilike na awakasirishe kwa kushindwa na aibu na hizaya, wapate kurejea nao wameemewa.

128 Huna lako katika ninayo wafanyia waja wangu, kwani mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Ama atawasamehe kwa Imani, au atawaadhibu kwa kuuwawa na hizaya na mateso ya Siku ya Kiyama, kwani hao ni madhaalimu.

129 Bila ya shaka vitu vyote vilioko katika mbingu na katika ardhi ni vya Mwenyezi Mungu peke yake, kwa kuviumba na kuvimiliki. Na Yeye ndiye Mwenye uwezo juu ya kila kitu, kila kitu kimo mikononi mwake. Yeye humsamehe ampendaye na akamuadhibu amtakaye. Lakini kusamehe kwake ndiko kulio karibu zaidi, na rehema yake ni ya kutarajiwa sana zaidi. Kwani Yeye hakika ni mwingi wa kusamehe na kurehemu

130 Enyi mlio amini! Mkipopesha msichukue katika deni ila rasilmali yenu tu. Msifanye kuzidisha juu ya deni faida ya kuzidi mwaka kwa mwaka ikawa kuzidi juu kwa juu. Msiyale mali ya watu kwa upotovu. Hakika nyinyi mtaongokewa na mtafuzu pindi mkiepukana na riba, ikiwa ndogo au kubwa.

131 Tahadharini na Moto ulio andaliwa kwa ajili ya makafiri kwa kujiepusha kutafuta kuihalalisha riba.

132 Na mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume katika kila wanacho amrisha na kila wanacho kikataza ili mpate kurehemeka duniani na Akhera.

133 Na kuweni wa mbele katika kutenda mema ili mpate kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye kumiliki mambo yenu yote, maghfira makubwa ya kufutiwa dhambi zenu, na Pepo yenye wasaa, na upana wake ni kama upana wa mbingu zote na ardhi. Hayo wametengenezewa wale wanao mcha Mwenyezi Mungu na wakaiogopa adhabu yake.

134 Hao wachamngu ndio wale wanao toa mali yao kwa kumridhi Mwenyezi Mungu wanapo kuwa na neema na wasaa, na pia wanapo kuwa na shida na dhiki na uzito, na wanazuia ghadhabu zao wanapo

135. Na ambao pindi wafanyapo uchafu au wakajidhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na wakamwomba msamaha kwa dhambi zao - na nani anaye futa dhambi isipo kuwa Mwenyezi Mungu? - na wala hawaendelei na waliyo yafanya na hali wanajua.¹³⁵

136. Hao malipo yao ni msamaha kwa Mola wao Mlezi, na Bustani zipitazo mito kati yake. Humo watadumu, na mwema mno ujira wa watendao.¹³⁶

137. Kabla yenu zimepita nyendo nyingi; basi tembeeni katika ulimwengu muangalie vipi ulikuwa mwisho wa wanao kanusha.¹³⁷

138. Hii ni bayana kwa watu wote, na ni uwongofu, na mawaidha kwa wachamngu.¹³⁸

139. Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini.¹³⁹

140. Kama yamekupateni majaraha, basi na hao watu wengine yamewapata majaraha mfano wa haya. Na siku za namna hii tunaweletea watu kwa zamu, ili Mwenyezi Mungu awapambanue walio amini na awateuwe miongoni mwenu mashahidi. Na Mwenyezi Mungu hawapendi madhaalimu,¹⁴⁰

141. Na pia ili Mwenyezi Mungu awasafishe walio amini na awafutilie mbali makafiri.¹⁴¹

142. Je! Mnadhani mtaingia Peponi na hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale miongoni mwenu walio pigana Jihadi, na hajawapambanua walio subiri?¹⁴²

kasirishwa wasiwaadhibu wale wanao wakosa, bali wanawasamehe walio watendea mabaya. Hao kwa haya huhisabiwa kuwa ndio watenda mema. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu huwalipa mema hao watenda mema na huwa radhi nao.

135 Watu hao nao pindi wakifanya makosa makubwa au dhambi ndogo tu, mara humkumbuka Mwenyezi Mungu na Utukufu wake, na adhabu zake na malipo yake mema, na rehema yake na ghadhabu zake. Tena hapo hujuta kwa waliyo tenda na wakaomba msamaha wake, na hapana anaye samehe madhambi ila Mwenyezi Mungu. Na hao wachamngu hawabaki kuendelea juu ya jambo baya na ilhali wanajua ubaya wake.

136 Basi hao wenye kusifika kwa sifa hizi ujira wao ni maghfira makubwa kutokana na Mola wao Mlezi, Mwenye kumiliki mambo yao yote, na Bustani zipitazo mito kati ya miti yake, na humo watadumu daima. Na hayo ni malipo ya neema kubwa ilioje kwa watendao amri za Mwenyezi Mungu.

137 Enyi Waumini, kabla yenu shani ya Mwenyezi Mungu imewapitia kaumu zilizo kadhibisha kwa mapuuza yao. Mwenyezi Mungu akawashika kwa madhambi yao. Basi zingatieni vipi yalikuwa matokeo ya vitendo vya walio kadhibisha.

138 Kwa kutajwa sifa za Waumini na kueleza shani ya Mwenyezi Mungu iliyo pita kwa walio kwisha tangulia lipo Bayana na Uwongozi kwa watu wafuate njia ya kheri, na kuwaachisha njia ya shari.

139 Wala nyinyi msilegelege mkadhoofika katika Jihadi Fi Sabili Llahi kwa yanayo kupateni, na wala msihuzunike kwa wanao uliwa miongoni mwenu, kwani nyinyi kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na Imani yenu na nguvu za Haki mnayo ipigania mko juu. Ushindi ni wenu ikiwa Imani yenu ni ya kweli, na maadamu mtadumu nayo.

140 Ingawa katika vita vya Uhud wameuwawa au kujuruhiwa vibaya baadhi yenu na kwa hayo mkaathirika nafsi zenu, lakini msilegee na kuhuzunika. Kwani hao makhasimu zenu yaliwapata kama hayo katika vita vya Badri. Nyakati za ushindi huendeshwa na Mwenyezi Mungu kwa watu kama apendavyo, pengine hawa hushinda, na pengine hawa, ili awatie mtihani na kuwajaribu Waumini, awateuwe wenye kusimama imara juu ya Imani yao, na apate kuwatukiza baadhi yao kwa kuwafisha mashahidi katika Sabili Llahi. Na Mwenyezi Mungu hawapendi washirikina wenye kudhulumu na wangashinda kwa kusaidiwa na wengineo.

141 Kwa huku kushindwa kwa muda, Mwenyezi Mungu anawasafisha jamaa Waumini, na anawat'ahirisha kutokana na wale wenye nyoyo mbaya na imani dhaifu, na wenye kueneza moyo wa kushindwa na wasiwasi; na kwa hivyo ndio anaung'olea mbali ukafiri na makafiri wenyewe pia.

142 Enyi Waumini! Msidhani kuwa mtaingia Peponi bila ya kubainika kati yenu wepi Mujahidiina, Wapigania Haki, wenye kusubiri na kuvumilia ambao wanat'ahirishwa na misukusuko na shida.

143. Na nyinyi mlikuwa mkitamani mauti kabla hamjakutana nayo. Basi sasa mmekwisha yaona na huku mnayatazama.¹⁴³

144. Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwisha pita kabla yake Mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma? Na atakaye geuka akarudi nyuma huyo hatamduru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wanao mshukuru.¹⁴⁴

145. Na haiwezi nafsi kuwa ife ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kama ilivyo andikwa ajali yake. Na mwenye kutaka malipo ya duniani tutampa; na mwenye kutaka malipo ya Akhera tutampa. Na tutawalipa wenye kushukuru.¹⁴⁵

146. Na Manabii wangapi walipigana na pamoja nao Waumini wengi wenye ikhlasi! Hawakufanya woga kwa yaliyo wasibu katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakudhoofika wala hawakuwa wanyonge. Na Mwenyezi Mungu huwapenda wanao subiri.¹⁴⁶

147. Wala kauli yao haikuwa ila ni kusema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu, na isimamisha imara miguu yetu na utunusuru tuwashinde kaumu ya makafiri.¹⁴⁷

148. Basi Mwenyezi Mungu akawapa malipo ya duniani na bora ya malipo ya Akhera. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao mema.¹⁴⁸

149. Enyi mlio amini! Ikiwa mtawat'ii walio kufuru watakurudisheni nyuma, na hapo mtageuka kuwa wenye kukhasiri.¹⁴⁹

150. Bali Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wenu, naye ndiye bora wa wasaidizi.¹⁵⁰

143 Nyinyi mlikuwa mkitaka kufa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kabla hamjayaona mauti na mkajua kitisho chake. Sasa basi nyinyi mmekwisha yaona mauti walipo uliwa ndugu zenu mbele yenu nanyi mnaangalia.

144 Katika vita vya Badri ulitoka uvumi kuwa ati Mtume Muhammad s.a.w. kauwawa. Baadhi ya Waislamu walidahadari wakaingia kiwewe wakataka kurtadi, kuuacha Uislamu. Mwenyezi Mungu aliwakaripia kwa kuwaambia: Muhammad si chochote ila ni Mtume tu, na kabla yake wamekufa Mitume mfano wake yeye. Naye atakufa kama walivyo kufa wao, na atapita kama wao walivyo pita. Je, akifa au akauliwa ndio mtarejea nyuma kwenye ukafiri wenu? Na mwenye kurejea kwenye ukafiri baada ya kwisha amini, basi hatomduru kitu Mwenyezi Mungu, ila atakuwa anajiduru nafsi yake kwa kujipeleka kwenye mateso. Na Mwenyezi Mungu atawalipa malipo mema wale wenye kusimama imara juu ya Uislamu, wenye kuishukuru neema yake.

145 Hayumkini mtu kufa ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Naye amekwisha viandikia viumbe ajali yao. Na atakaye starehe ya dunia Mwenyezi Mungu atampa, na atakaye malipo ya Akhera atayapata. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wanao shukuru neema yake wakamt'ii kwa aliyi waamrisha ikiwa ni kupigana Jihadi au mengineyo.

146 Na Manabii wangapi wamepigana vita na pamoja nao Waumini wengi wenye ikhlasi kwa Mola wao Mlezi! Nyoyo zao hazikuingia woga, wala azma zao hazikudahadari, wala hawakuwanyenyekea maadui zao kwa sababu ya masaibu yaliyo wapata katika Sabili Llahi, Njia ya Mwenyezi Mungu. Haya ni kwa sababu wamo katika ut'iifu wake, na Mwenyezi Mungu huwalipa wanao vumilia ikiwafika balaa.

147 Na kauli yao vilipo kuwa vita vikali haikuwa ila kusema: Mola wetu Mlezi! Tusamehe dhambi zetu kubwa na ndogo. Na tusimamisha imara katika midani za vita, na utunusuru na hawa maadui wa Dini yako, wenye kukukanya Wewe na ujumbe wa Mtume wako.

148 Mwenyezi Mungu akawapa ushindi na tawfiqi katika dunia, na akawadhaminia malipo mema kwa Akhera. Na Mwenyezi Mungu huwalipa wale wafanyao vitendo vyema.

149 Enyi mlio amini! Mkiwat'ii maadui zenu makafiri, walio tangaza ukafiri wao au wakauficha, kwa hayo wanayo kuitieni kwa maneno au vitendo, watakuja kugeuzeni muingie ukafirini. Na hapo tena itakuwa mmekhasiri dunia na Akhera.

150 Mwenyezi Mungu ndiye wa kukunusuru, basi msiwaogope hao binaadamu wenzenu, kwani

151. Tutazitia khofu nyoyo za walio kufuru kwa vile walivyo mshirikisha Mwenyezi Mungu na washirika ambao hakuwateremshia hoja yoyote. Na makaazi yao ni Motoni; na maovu yaliyoje maskani ya wenye kudhulumu!¹⁵¹

152. Na Mwenyezi Mungu alikutimilizieni miadi yake, vile mlivyo kuwa mnawauwa kwa idhini yake, mpaka mlipo legea na mkazozana juu ya amri, na mkaasi baada ya Yeye kukuonyesheni mliyo yapenda. Wapo miongoni mwenu wanao taka dunia, na wapo miongoni mwenu wanao taka Akhera. Kisha akakutengeni nao (maadui) ili akujaribuni. Naye sasa amekwisha kusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila juu ya Waumini.¹⁵²

153. Pale mlipo kuwa mkikimbia mbio wala hamumsikilizi yeyote, na Mtume anakuiteni, yuko nyuma yenu. Mwenyezi Mungu akakupeni dhiki juu ya dhiki, ili msisitike kwa yaliyo kukoseeni wala kwa yaliyo kusibuni. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayo yatenda.¹⁵³

154. Kisha baada ya dhiki alikuteremshieni utulivu - usingizi ambao ulifunika kundi moja kati yenu. Na kundi jengine nafsi zao ziliwashughulisha hata wakamdhania Mwenyezi Mungu dhana isiyo kuwa ya haki, dhana ya kijinga. Wakisema: Hivyo tuna lolote sisi katika jambo hili? Sema: Mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Wanaficha katika nafsi zao wasiyo kubainishia. Wanasema: Lau ingelikuwa tuna lolote katika jambo hili tusinge uliwa hapa. Sema: Hata mngeli kuwa majumbani mwenu, basi wangeli toka walio andikiwa kufa, wakenda mahali pao pa kuangukia wafe. (Haya ni hivyo) ili Mwenyezi Mungu ayajaribu yaliyomo vifuani mwenu, na asafishe yaliyomo nyoyoni mwenu. Na Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo vifuani.¹⁵⁴

Mwenyezi Mungu ndiye mboru wa kunusuru.

151 Yasikutieni unyonge yaliyo kupateni siku ya Uhud. Sisi tutaingiza khofu na vitisho katika nyoyo za maadui zenu kwa kuwa wao wamemshirikisha Mwenyezi Mungu na miungu mengine ambayo Mwenyezi Mungu hakuwateremshia hoja yoyote. Kwani Miungu hiyo hainafiishi wala haidhurishi kitu. Na makao yao yatakuwa Motoni Akhera, na maovu mno hayo makao ya madhaalimu.

152 Nusura ya Mwenyezi Mungu ni jambo la hakika ya kweli. Mwenyezi Mungu ametimiza miadi yake kuwa alikupeni ushindi pale mara ya kwanza mlipo wauwa maadui wengi kwa radhi yake; mpaka yalipo dhoofika maoni yenu katika vita na mkakhitalifiana kuifahamu amri ya Nabii aliyo kupeni msiondoke kwenye vituo vyenu. Baadhi yenu mkaacha vituo vyenu mlipo ona mnashinda, na wengine wakabaki mpaka mwisho. Kikundi kimoja kikaasi amri ya Mtume kikenda kuwania ngawira baada ya kwisha kuonyesha mkipendacho, nao ni ushindi. Mkawa makundi mawili, wanao taka raha ya dunia, na wanao taka malipo ya Akhera. Hivyo kuwa hivyo Mwenyezi Mungu akaondoa kwenu nuSura yake, mkashindwa, ili akujaribuni, atambulikane mwenye ikhlasi na asiye kuwa nayo. Lakini sasa amekusameheni kwa kuwa mmejuta. Na Mwenyezi Mungu ana fadhila kwenu kwa kukusameheni na kukubali toba yenu.

153 Enyi Waumini! Hebu ikumbukeni hali yenu wakati ule mlipo kuwa mkitoka mbio wala hamumsikii mtu kwa shida ya kukimbia; na Mtume anakuiteni nyuma yenu mrejee. Mwenyezi Mungu akakujazini huzuni ya kufudikiza kama wingu lilio funika nafsi zenu, ili msisitike kwa ngawira mlizo zikosa wala kushindwa kuliko kusibuni. Na Mwenyezi Mungu anajua vyema makusudio yenu na vitendo vyenu.

154 Kisha Mwenyezi Mungu baada ya dhiki akakupeni neema ya utulivu, ambao ulidhahiri kwa usingizi ulio wafunika wale walio wa kweli katika Imani yao na kumtegemea kwao Mwenyezi Mungu. Ama kile kikundi kingine, hamu yao ni juu ya nafsi zao tu hawana jenginelu; kwa hivyo wakamdhania Mwenyezi Mungu dhana mbovu za kijahiliya, wakisema kwa kuchukiwa: Tumepata ushindi wowote sisi huo tulio ahidiwa? Sema ewe Nabii: Mambo yote ya kushinda na kushindwa yako kwa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye mwenye kuyaendesha mambo kwa waja wake pindi wao wakichukua khatua za ushindi, au wakifanya mambo ya kusabibisha kushindwa. Na wao wanapo sema hayo wana jambo wanalo lificha katika nafsi zao, wala hawalidhihirishi. Kwani wao husema: Ingeli kuwa sisi tuna khiari yetu tusingeli toka, basi tusingeli shindwa. Waambie: Hata mngeli kuwa ndani ya majumba yenu na kama wapo walio

155. Hakika wale walio rudi nyuma miongoni mwenu siku yalipo pambana majeshi mawili, Shet'ani ndiye aliye watelezesha kwa sababu ya baadhi ya makosa waliyo yafanya; na Mwenyezi Mungu amekwisha wasamehe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mpole.¹⁵⁵

156. Enyi mlio amini! Msiwe kama wale walio kufuru na wakawasema ndugu zao walipo safiri katika nchi au walipo kuwa vitani: Wangeli kuwa kwetu wasingeli kufa na wasingeli uwawa. Ili Mwenyezi Mungu afanye hayo kuwa ni majuto katika nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu huhuisha na hufisha. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona myatendayo.¹⁵⁶

157. Na pindi mkiuliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu, au mkifa, hakika maghfira na rehema zitokazo kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko yote wanayo yakusanya.¹⁵⁷

158. Na mkifa au mkiuliwa ni kwa Mwenyezi Mungu ndio mtakusanywa.¹⁵⁸

159. Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungesi kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombe maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea.¹⁵⁹

160. Akikunusuruni Mwenyezi Mungu hapana wa kukushindeni, na akikutupeni ni nani, basi, baada yake Yeye ataye kunusuruni? Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.¹⁶⁰

andikiwa kuuliwa basi hapana shaka wangeli toka mpaka pahala pao pa kufa wakauliwa. Na Mwenyezi Mungu amefanya aliyo yafanya hapo Uhud kwa maslaha makubwa, ili apate kutoa ndani yenu ikhlasi, na azitahirishe nyoyo zenu. Na Mwenyezi Mungu anayajua vilivyo yaliyo fichika ndani ya nyoyo zenu. 155 Enyi jamaa wa Kiislamu! Wale miongoni mwenu walio acha kusimama imara pale pahali pao walipo wekwa wasimame hakika ni Shetani ndiye aliye wavuta kwenye utelezi na kukosea kwa sababu ya makosa yao kumkhaalifu Mtume. Lakini Mwenyezi Mungu amekwisha wasamehe, kwani Yeye ni mwingi wa maghfira, na mwingi wa upole.

156 Enyi mlio amini! Msiwe kama walio kufuru wakasema, kwa mintarafu ya wenzao wanapo ondoka kwenda safarini kutafuta maisha wakafa, au wakenda vitani wakauwawa: Lau wangeli bakia nasi hapa wasingeli kufa, na wasingeli uwawa. Mwenyezi Mungu amejaalia kauli yao hiyo na dhana yao iwe ni majuto ya nyoyoni mwao. Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuhuisha na Mwenye kufisha, na kudra ya kila kitu imo mikononi mwake. Yeye anayajua yote myatendayo, ya kheri na shari. Na Yeye ndiye wa kukulipeni.

157 Na mkiuwawa katika Jihadi au mkafa wakati huo, basi hayo hakika ni kupata maghfira ya Mwenyezi Mungu kufutiwa dhambi zenu, na kupata rehema itokayo kwake. Hayo ni bora kuliko starehe za dunia ambazo mnge zikusanya lau mgeli bakia.

158 Na lau mtakufa au mtauliwa katika Jihadi hazitopotea bure a'mali zenu, kwani mtakusanywa kwa Mwenyezi Mungu akulipeni kwa Jihadi yenu na ikhlasi yenu.

159 Ilikuwa ni rehema ya Mwenyezi Mungu kwako wewe (Muhammad) na kwao (Waumini) kwa kuwa wewe umekuwa laini kwao wala hukuwatolea neno la ukali kwa kukosea kwao. Na lau kuwa wewe ungesi kuwa unawachukulia kwa ukavu, na moyo mgumu wangeli kukimbia. Basi nawe yapuuze makosa yao, na waombe msamaha, na ushauriane nao katika mambo ili upate maoni yao katika mambo ambayo siyo ulio teremshiwa ufunuo, Wahyi. Ukisha funga azimio lako juu ya jambo baada ya kushauriana, basi endelea nalo na huku ukimtegemea Mwenyezi Mungu. Kwani Mwenyezi Mungu humpenda anaye mwakilisha mambo yake Yeye.

160 Mwenyezi Mungu akikuungeni mkono kwa nuSura yake, kama ilivyo tokea siku ya Badri, hatokushindeni yeyote. Na akikuacheni mkono kwa kuwa nyinyi hamkuchukua khatua zifaazo za ushindi, kama yaliyo pita siku ya Uhud, basi hamtakuwa na wa kukunusuruni mwengine. Na ni juu ya Mwenyezi Mungu peke yake ndio yawapasa Waumini wategemeze mambo yao yote.

161. Na haiwezekani kwa Nabii yeyote kufanya khiyana. Na atakaye fanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyo yafanyia khiyana, kisha kila mtu atalipwa kwa aliyo yachuma, kwa ukamilifu; wala hawatadhulumiwa.¹⁶¹

162. Je! Aliye yafuata ya kumridhisha Mwenyezi Mungu ni kama yule aliye stahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na makaazi yake yakawa Jahannamu? Napo ni mahala pabaya pa kurejea.¹⁶²

163. Hao wana vyeo mbali mbali kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona yote wayatendayo.¹⁶³

164. Hakika Mwenyezi Mungu amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyo waletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, anaye wasomea Aya zake, na anawatakasa, na anawafunza Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya hapo walikuwa katika upotovu ulio wazi.¹⁶⁴

165. Nyinyi - ulipo kusibuni msiba ambao nyinyi mmekwisha watia mara mbili mfano wa huo - mnasema: Umetoka wapi huu? Sema: Huo umetoka kwenu wenyewe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.¹⁶⁵

166. Na yaliyo kusibuni siku yalipo pambana majeshi mawili yalikuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ili awajue Waumini.¹⁶⁶

167. Na ili awapambanue walio kuwa wanaafiki, wakaambiwa: Njooi mpigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu au linden. Wakasema: Tungeli jua kuna kupigana bila ya shaka tungeli kufuateni. Wao siku ile walikuwa karibu na ukafiri kuliko Imani. Wanasema kwa midomo yao yasiyo kuwamo nyoyoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anajua kabisa wanayo yaficha.¹⁶⁷

161 Haisihi kuwa Nabii yeyote *kukhuni* katika ngawira kama walivyo eneza kwa uzushi wanaafiki waongo. Kwani khiyana ni kinyume na Unabii. Basi isikupitikieni dhana hiyo. Na mwenye kukhuni atakuja Siku ya Kiyama na mzigo wa dhambi wa khiyana yake, tena kila nafsi italipwa ilicho tenda, kwa ukamilifu. Na wala hawatadhulumiwa kwa kupunguzwa thawabu zao wala kuzidishiwa adhabu yao.

162 Hawawezi kuwa sawa, anaye piga mbio kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu kwa vitendo na ut'iifu, na yule anaye stahiki ghadhabu kuu ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya uasi wake. Na mwenye kuasi ataishia Jahannamu, na kuovu kulioje huko!

163 Makundi mawili hayo hayawi sawa, bali yametafautiana mbele ya Mwenyezi Mungu kwa daraja mbali mbali. Na Mwenyezi Mungu anazijua vyema hali zao na daraja zao, na atawalipa kwa mujibu wake.

164 Mwenyezi Mungu amewafadhili Waumini wale wa mwanzo walio kuwa na Nabii s.a.w. kwa kuwapelekea Mtume aliye tokana na wao wenyewe, akiwasomea Aya za Kitabu, na akiwat'ahirisha na itikadi mbovu, akiwafundisha Qur'ani na Sunna za Mtume, na ilhali kabla ya kuletwa Mtume, walikuwa katika ujinga na ubabaishi na upotovu.

165 Hivyo mnapiywa na mshangao na kuemewa pale yalipo kupateni siku ya Uhud masaibu ambayo nyinyi mlikwisha wapa maadui mara mbili mfano wa hayo katika siku ya Badri, hata mnasema kwa mastaaajabu: Yamekuwa je mauwaji haya na kushindwa huku, na sisi ni Waislamu na Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko nasi? Sema: Yaliyo kupateni yametokana na nafsi zenu kwa vile mliyoy mikhailifu Mtume. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu, naye amekulipeni kwa mujibu wa mliyoy tenda.

166 Enyi Waumini! Yaliyo kusibuni lilipo pambana jeshi lenu na jeshi la Washirikina katika Uhud yametokana kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu, na ili awadhahirishie watu Imani ya Waumini ya kweli aliyo ifunza.

167 Na hayo ili pia udhahiri unaafiki wa wanaafiki. Nao hawa ni wale walipo kuwa wanaondoka wanaacha vita wakaambiwa: Njooi mpigane kwa kumt'ii Mwenyezi Mungu, au kwa ajili ya kujilinda nafsi zenu. Wakasema: Lau kuwa tunajua kuwa mtakutana na vita, tungeli kwenda nanyi. Na wao walipo sema kauli hiyo walikuwa karibu zaidi na ukafiri kuliko Imani. Wanasema kwa midomo yao: Huko hakuna vita. Na hali wanaitakidi ndani ya nyoyo zao kuwa vita kweli vitakuwepo. Na Mwenyezi Mungu anajua vyema

168. Hao ndio walio waambia ndugu zao na wao wenyewe wakakaa kitako: Lau wengeli tut'ii wasingeli uliwa. Sema: Ziondoleeni nafsi zenu mauti kama mnasema kweli.¹⁶⁸

169. Wala kabisa usiwadhania walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi.¹⁶⁹

170. Wanafurahia aliyo wapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake, na wanawashangilia wale ambao bado hawajajiunga nao, walio nyuma yao, ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.¹⁷⁰

171. Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa Waumini,¹⁷¹

172. Walio mwitikia Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya kwisha patwa na majaraha - kwa walio fanya wema miongoni mwao na wakamchamngu utakuwa ujira mkubwa.¹⁷²

173. Walio ambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa.¹⁷³

174. Basi wakarudi na neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa, na wakafuata yanayo mridhi Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu.¹⁷⁴

175. Hakika huyo ni Shet'ani anawatia khofu marafiki zake, basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini.¹⁷⁵

unaafiki wanao uficha, kwani Yeye anajua matokeo ya siri zao.

168 Na hao ndio walio baki nyuma wesende vitani wakakwepa, na wakasema kwa mintarafu ya ndugu zao walio toka wakauliwa: Lau wangeli tufuata sisi wakakaa nyuma kama tulivyo kaa sisi wangeli okoka kama tulivyo okoka. Waambie: Zizuieni nafsi zenu basi zisife, kama mnasema kweli kuwa hadhari inazuia kadari.

169 Wala usidhani kabisa kuwa walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni maiti, bali hao wahai kwa uhai anao ujua Mwenyewe Mwenyezi Mungu, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi, riziki njema anayo ijua Yeye.

170 Nyuso zao zinameremeta kwa furaha na bishara kwa fadhila ya pekee aliyo wapa Mwenyezi Mungu, na wanawafurahia ndugu zao ambao walio waacha duniani wangali wahai, wanashika mwendo wa Imani na Jihadi, na ya kwamba hapana khofu juu yao kupata lolote la karaha wala si wenye kuhuzunika kwa kumkosa mpendwa.

171 Nyuso za Mashahidi zinameremeta kwa neema ya kufa shahidi na neema ya Pepo, na ubora wa karama, na ya kwamba haupotei ujira wa Waumini.

172 Waumini hao ni wale ambao wameitikia wito wa Mtume wa kuanza upya Jihadi baada ya pigo kubwa walilo lipata katika vita vya Uhud. Kwa hivyo basi wakawa ni wenye kutenda wema, na wakajilinda na kuasi amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Basi wakastahiki ujira mkubwa katika Nyumba ya Malipo na Neema.

173 Hao ndio walio tiwa khofu na watu kwa kuwaambia: Maadui zenu wamekusanya jeshi kubwa kukupigeni, basi waogopeni. Na wao hawakudhoofika wala hawakulegea, bali walizidi Imani ya Mwenyezi Mungu na wakawa na moyo kuwa atawanusuru. Jawabu yao ikawa: Mwenyezi Mungu anatutosheleza. Yeye ndiye aliye tawala mambo yetu. Na Yeye ndiye anaye tegemezwa mambo yote.

174 Kisha wakatoka kwenda kwenye Jihadi na kupambana na hilo jeshi kubwa, lakini washirikina wakaingiwa na woga wakakimbia. Wakarejea Waumini kuwa wameshinda kwa neema ya salama ilhali wao wana hamu ya Jihadi, na wana malipo na thawabu na fadhila ya Mwenyezi Mungu kwao kwa vile kutia kitisho katika nyoyo za maadui zao, na wao wasipatikane na maudhi yoyote. Waliitafuta radhi ya Mwenyezi Mungu, na wao wakaistahiki fadhila yake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa.

175 Mwenyezi Mungu Aliye takasika anawabainishia Waumini kwamba hao wanao kutieni khofu kuogopa kupambana na maadui zenu si lolote ila ni vibaraka wa Shetani anaye watia khofu wafwasi wake awafanye woga. Na nyinyi si katika hao. Basi msiridhie kutishwa, bali mkhofuni Mwenyezi Mungu

176. Wala wasikuhuzunishe wale wanao kimbilia ukafirini. Hakika hao hawamduru kitu Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anataka asiwawekee sehemu yoyote katika Akhera, na yao wao adhabu kubwa.¹⁷⁶

177. Hakika wale walio nunua ukafiri kwa Imani hawatamduru kitu Mwenyezi Mungu, na yao wao ni adhabu chungu.¹⁷⁷

178. Wala wasidhani wale wanao kufuru kwamba huu muhula tunao wapa ni kheri yao. Hakika tunawapa muhula wazidi madhambi. Na yao wao ni adhabu ya kuwadhalilisha.¹⁷⁸

179. Haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwaacha Waumini katika hali mliyo nayo mpaka apambanue wabaya na wema. Wala haiwi kwa Mwenyezi Mungu kukujuulisheni mambo ya ghaibu. Lakini Mwenyezi Mungu humteua katika Mitume wake amtakaye. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mitume yake. Na mkiamini na mkamchamngu mtakuwa na ujira mkubwa.¹⁷⁹

180. Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake kuwa ni kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao. Watafungwa kongwa za yale waliyo yafanyia ubakhili Siku ya Kiyama. Na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote myatendayo.¹⁸⁰

181. Mwenyezi Mungu amekwisha sikia kauli ya walio sema: Mwenyezi Mungu ni masikini, na sisi ni matajiri. Tumeyaandika waliyo yasema, na pia kuwauwa kwao Manabii bila ya haki, na tutawaambia Siku ya Kiyama: Onjeni adhabu ya kuungua.¹⁸¹

peke yake kama nyinyi mna Imani ya kweli, na mnasimamia kutimiza yanayo lazimishwa na Imani hiyo. 176 Ewe Nabii! Usihuzunike ukiwaona wale ambao wanazidi ukafiri, na wanawania kuzidisha maovu. Hao hawamletei Mwenyezi Mungu madhara yoyote, kwani Yeye ni Mwenye nguvu juu ya waja wake. Bali Mwenyezi Mungu anataka wasiwe na sehemu yoyote katika thawabu za Akhera, na juu ya kukosa kwao thawabu hizo njema watapata adhabu kubwa.

177 Hakika watu hao walio khiari ukafiri badala ya Imani, wakatafuta ukafiri na wakaacha Imani, hawatamduru kitu Mwenyezi Mungu, na watapata Akhera adhabu kali ya kutia uchungu mkubwa.

178 Wasidhani hao makafiri kuwa vile kuwapururia tunapo wakunjulia umri wao, na tukawapa njia za starehe katika maisha yao ya duniani, kuwa ndio kheri yao. Kwani kuwaongezea umri na kuwakunjulia riziki huwapelekea kudumu na kuchuma madhambi na kuzidi kustahiki adhabu ya kuwafedhehesha aliyo waandalia Mwenyezi Mungu.

179 Haiwi kuwa Mwenyezi Mungu akuacheni enyi jamaa Waumini katika hali hii hii mliyo nayo ya mchanganyiko wa Muumini na mnaafiki, mpaka awatenganishe baina yenu kwa misukosuko na taabu ili mumwone mnaafiki khabithi na Muumini mwema. Wala sio mwendo wa Mwenyezi Mungu kumjuulisha yeyote katika viumbe vyake khabari za ghaibu. Walakini Mwenyezi Mungu humteua katika Mitume yake ampendaye akamjuvya anacho kitaka katika mambo yake ya ghaibu. Na nyinyi mkiamini na mkamcha Mola wenu Mlezi kwa kujilazimisha kumt'ii atakutieni katika Pepo iwe ndio malipo. Na hayo ndio malipo yaliyo bora na makubwa kabisa.

180 Wasidhani wanao fanya ubakhili kwa mali aliyo waneemesha Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake, na hawayatoi katika yaliyo waajibu na njia za kheri, kuwa ubakhili huo ni kheri yao. Bali hiyo ni shari yenye matokeo mabaya juu yao. Watalipwa malipo maovu kabisa Siku ya Kiyama, na adhabu itawaganda kama kongwa au mnyororo aliyo fungwa nayo mfungwa shingoni mwake. Kila kiumbe kinamnyenyekea Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la*, naye ndiye Mmiliki wao, na Yeye Aliye takasika anajua kila mnacho kitenda, na atakulipeni kwacho.

181 Juu ya kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kumiliki kila kiliomo mbinguni na ardhini na Yeye ndiye mrithi wa vyote, wamesema baadhi ya Mayahudi kwa kejeli: Mwenyezi Mungu ni fakiri, ndiyo akatutaka tutoe, na sisi ni matajiri tukitoe au tusitoe. Mwenyezi Mungu amekwisha isikia kauli yao hiyo, na ameisajili dhidi yao, kama alivyo sajili kuwauwa kwao Manabii kwa dhulma na ukhalifu na uadui. Naye atawaambia Siku ya Kiyama: Onjeni adhabu ya Moto unao waka!

182. Haya ni kwa sababu ya iliyo tanguliza mikono yenu, na kwamba Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja,¹⁸²

183. Walio sema: Mwenyezi Mungu ametuahidi tusimuamini Mtume yeyote mpaka atuletee kafara inayo teketezwa na moto. Waambie: Walikujieni Mitume kabla yangu kwa hoja zilizo wazi na kwa hayo mnayo sema, basi kwa nini mkawauwa ikiwa mlikuwa wakweli?¹⁸³

184. Na wakikukanusha basi walikanushwa Mitume wengine kabla yako walio kuja na hoja waziwazi na Vitabu vyenye hikima, na Kitabu chenye nuru.¹⁸⁴

185. Kila nafsi itaonja mauti. Na bila ya shaka mtapewa ujira wenu kaamili Siku ya Kiyama. Na atakaye epushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu. Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu.¹⁸⁵

186. Hapana shaka yoyote mtapata misukosuko katika mali zenu na nafsi zenu, na bila ya shaka yoyote mtasikia udhia mwingi kutokana na walio pewa Kitabu kabla yenu na wale walio shiriki. Na ikiwa mtasubiri na mkamchamngu basi hakika hayo ni katika mambo ya kuazimia.¹⁸⁶

187. Na pale Mwenyezi Mungu alipo fungamana na walio pewa Kitabu kuwa: Lazima mtawabainishia watu, wala hamtokificha, walikitupa nyuma ya migongo yao, na wakanunua kwacho thamani duni. Basi ni kiovu hicho walicho nunua.¹⁸⁷

188. Usiwadhania kabisa wale wanao furahia waliyo yafanya, na wakapenda kusifiwa kwa wasiyo yatenda, usiwadhania kuwa watasalimika na adhabu. Yao wao ni adhabu chungu.¹⁸⁸

182 Na hiyo adhabu ni kwa dhambi zao walizo zitenda wenyewe, na malipo ya Mwenyezi Mungu hayawi ila ni kwa uadilifu, wala Yeye kabisa hawadhulumu waja wake.

183 Hao ndio walio sema: Mwenyezi Mungu ametuamrisha katika Taurati tusimfuata Mtume yeyote ila akileta dalili ya ukweli wake kwa kutuletea kitu cha kumkurubisha kwenye radhi ya Mwenyezi Mungu, na uteremke moto kutoka mbinguni ukile hicho kitu. Ewe Nabii! Waambie: Hakika Mitume kutoka kwa Mwenyezi Mungu wamekwisha kukujieni kabla yangu, wakaja na dalili zilizo wazi, na wakaja na hayo mnayo yasema. Na juu ya hayo mliwakadhibisha na mkawauwa. Kwa nini mkafanya hayo kama nyinyi ni wasema kweli katika ahadi yenu ya Imani yanapo timia mnayo yataka?

184 Ikiwa *watakukadhibisha*, Ewe Nabii, wewe usisikitike. Kabla yako wamekutangulia wengi walio kadhibishwa na watu wao kwa chuki na inda, juu ya kuwa walikuja na dalili zilizo nyooka, na Vitabu vya mbinguni vyenye kuthibitisha ukweli wa Ujumbe wao.

185 Hapana hivi wala hivi, kila nafsi lazima ionje kufa. Na ikiwa hapa duniani mtapata machungu basi Siku ya Kiyama mtalipwa thawabu kwa ukamilifu. Na mwenye kuukaribia Moto akaepushwa nao basi huyo amefuzu. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe yenye kupita, haina dawamu.

186 Kuweni na yakini, enyi Waumini, kuwa mtapata mitihani na majaribio katika mali yenu, kwa kupungua, kutoa au kunyang'anywa, na katika nafsi zenu kwa Jihadi au kuuwawa au kwa maradhi na machungu. Na kadhaalika mtasikia kutokana na Mayahudi na Wakristo na mapagani, washirikina, matusi na uchokozi wa kukuudhini. Na mkiyakaabili hayo kwa kuvumilia na kumcha Mwenyezi Mungu basi itakuwa ni katika mambo mema yanayo wajibika kuazimia kuyatimiliza.

187 Ewe Nabii! Kumbuka na utaje pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi madhbuti kwa Watu wa Kitabu, kuwa wayaeleze wazi maana ya Kitabu chao, na wala wasiwafiche watu chochote, na wao wakakitupilia mbali nyuma ya migongo yao, na badala yake wakatafuta starehe za dunia. Na starehe za dunia kama zitakavyo kuwa ni kitu chenye thamani duni kabisa kulinganisha na uwongofu na uwongozi. Ama wamejua kutenda uovu! (Hayo yalikuwa zamani na bado yanaendelea. Kuficha na kugeuza na kupotosha Biblia hakusiti. Vipo vitabu vyao vinavyo itwa "Apokrifa", maana yake "Vilivyo fichwa", kwa kuwa hivyo ni marfuku visisomwe ila na mapadri tu, na vingine vimeteketewa. Miongoni mwa hivyo ni Injili ya Barnaba.)

188 Usiwadhania kabisa kuwa wataepuka adhabu wale wanao tenda maovu, na wakapenda kusifiwa kwa

189. Na Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.¹⁸⁹

190. Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili,¹⁹⁰

191. Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto.¹⁹¹

192. Mola wetu Mlezi! Hakika unaye mtia Motoni umemhizi; na walio dhulumu hawana wasaidizi¹⁹²

193. Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumemsikia mwenye kuita akiitia Imani kwamba: Muaminini Mola wenu Mlezi; nasi tukaamini. Basi tusamehe madhambi yetu, na utufutie makosa yetu, na utufishe pamoja na watu wema.¹⁹³

194. Mola wetu Mlezi! Na utupe uliyo tuahidi kwa Mitume wako, wala usituhizi Siku ya Kiyama. Hakika Wewe huvunji miadi.¹⁹⁴

195. Mola Mlezi wao, akayakubali maombi yao akajibu: Hakika sipotezi kazi ya mfanya kazi miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke, kwani ni nyinyi kwa nyinyi. Basi walio hama, na walio tolewa makwao, na wakateswa katika Njia yangu, na wakapigana, na wakauliwa, kwa yakini Mimi nitawafutia makosa yao, na kwa yakini nitawaingiza katika Mabustani yanayo pita mito kati yake. Hayo ndiyo malipo yanayo toka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu kwake yapo malipo mema kabisa.¹⁹⁵

wasilo lifanya. Shani yao hao ni kujifungia mlango wa Imani na Haki, kama Mayahudi. Nao watapata adhabu chungu Siku ya Kiyama.

189 Mwenyezi Mungu pekee ndiye Mwenye mamlaka ya kila jambo la mbinguni na duniani. Naye ni Muweza wa kila kitu. Atawashika wenye dhambi kwa dhambi zao, na atawalipa thawabu watendao mema kwa wema wao.

190 Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na viliomo ndani yao kwa vile vilivyo umbwa tangu mwanzo na mipango yake, na kukhitalifiana usiku na mchana kwa mwangaza na giza, kwa urefu wake na ufupi, zipo dalili na ishara zilizo wazi kwa watu wenye akili na kutambua za kuthibitisha Umoja wa Mwenyezi Mungu na Uwezo wake. (*Tazama Maelezo 3:190*)

191 Ni shani ya wenye akili kuwa kila pahali wao wanahudhurisha katika nafsi zao adhama na utukufu wa Mwenyezi Mungu, wakiwa wamesimama au wamekaa au wamejinyoosha kitandani, na wanazingatia uumbaji wa mbingu na ardhi pamoja na viliomo ndani yake, na huku wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuumba haya ila kwa hikima uliyo ikadiria. Na Wewe umetakasika na kila upungufu. Bali umeumba hivi vyote kuwa ni dalili ya kudra yako, na ishara ya upeo wa hikima yako. Utuhifadhi na adhabu ya Moto kwa kutuwezesha kukut'ii.

192 Ewe Muumba wetu, na Mwenye kutusimamia mambo yetu, na Mlinzi wetu! Hakika mwenye kustahiki Moto na ukamuingiza, basi umempa hizaya. Na mwenye kudhulumu akastahiki Moto hana wa kumnusuru nao.

193 Ewe Muumba wetu, na Mwenye kutusimamia mambo yetu, na Mlinzi wetu! Hakika sisi tumemsikia Mtume wako akiita watu wakuamini Wewe, nasi tukamt'ii na tukamuamini. Ewe Mola wetu Mlezi! Tughufirie madhambi yetu makubwa, na tufutie maovu yetu madogo madogo, na baada ya kufa kwetu tujaalie tuwe pamoja na waja wako walio bora.

194 Ewe Muumba wetu, na Mwenye kutusimamia mambo yetu, na Mlinzi wetu! Tupe uliyo tuahidi kwa ndimi za Mitume yako, nayo ni ushindi na kuungwa mkono duniani. Wala usituingize Motoni ukatuhizi Siku ya Kiyama. Shani yako ni kuwa huendi kinyume na miadi yako.

195 Mola wao Mlezi aliwaitikia dua yao, akiwabainishia kuwa Yeye hampotezei mtendaji thawabu za vitendo vyake, sawa sawa akiwa mwanamume au mwanamke, kwani mwanamke anatokana na mwanamume, na mwanamume anatokana na mwanamke. Basi wale walio hajiri, wakahama, wakagura,

196. Kabisa kusikudanganye kubakia kutangatanga kwa walio kufuru katika nchi.¹⁹⁶

197. Hiyo ni starehe ndogo. Kisha makaazi yao yatakuwa Jahannamu. Na ni mahali pabaya mno pa kupumzikia.¹⁹⁷

198. Lakini walio mcha Mola wao Mlezi watapata Mabustani yanayo pita mito kati yake. Watadumu humo. Hayo ni makaribisho yao yatokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na vilioko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kwa watu wema.¹⁹⁸

199. Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu wapo wanao muamini Mwenyezi Mungu na yaliyo teremshwa kwenu na yaliyo teremshwa kwao, wakimnyenyekea Mwenyezi Mungu. Hawabadili Aya za Mwenyezi Mungu kwa thamani duni. Hao wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.¹⁹⁹

200. Enyi mlio amini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa.²⁰⁰

wanatafuta radhi ya Mwenyezi Mungu, na wakatolewa makwao, na wakapata mateso katika Sabili Llahi, Njia ya Mwenyezi Mungu, wakapigana vita, na wakakhatirisha kuuwawa, bali wakauliwa walio uliwa, Mwenyezi Mungu amejilazimisha Mwenyewe kuwasamehe madhambi yao, na kuwatia kwenye Mabustani yenye kupita kati yake mito, kuwa ni malipo matukufu yaliyo bora kutokana na Mwenyezi Mungu. Na kwa Mwenyezi Mungu peke yake, ndio yako malipo mazuri.

196 Usiathirike, ewe Nabii, kwa kuwaona makafiri wamo katika starehe za neema, na biashara na uchumi unawaendea, wakienda huku na huku katika nchi.

197 Hizo ni starehe za kupita njia, na kila kipitacho ni duni. Kisha marejeo ya daima watayo ishia ni Jahannamu. Na hapana makaazi maovu kama Jahannamu.

198 Hayo ndiyo malipo ya makafiri. Ama walio muamini Mwenyezi Mungu wakamwogopa Mola wao Mlezi watapata Mabustani yalitayo mito kati yake, watadumu humo daima, kuwa ni wageni walio pokewa kwa ukarimu na Mwenyezi Mungu, *Subhanahu*, Aliye takasika. Na yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ndio mazuri kwa watu wema kuliko hayo wanayo starehea makafiri ambayo yataondoka, hayadumu.

199 Hakika baadhi ya Watu wa Kitabu, Mayahudi na Wakristo, wanamuamini Mwenyezi Mungu, na wanaamini aliyote teremshiwa Nabii Muhammad s.a.w. na walio teremshiwa Mitume walio kuwa kabla yake. Utawaona wanamnyenyekea Mwenyezi Mungu, na wanakuwa wanyonge kwake, wala hawabadilishi bayana zilizo dhaahiri kwa ajili ya kutafuta pato la duniani. Hilo nalingawa kubwa ni kitu duni. Hawa wana malipo ya ukamilifu kwa Mola wao Mlezi katika makaazi ya kuridhisha. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu, hashindwi kuzidhibiti 'amali zao zote na kuwahisabia. Yeye ni Muweza wa hayo na malipo yake yatawafika bila ya shaka.

200 Enyi mlio amini! Shikamaneni na subira, na mwashinde maadui zenu katika kusubiri. Na kaeni macho kuulinda mipaka, na mkhofini Mola Mlezi wenu. Katika haya yote ndio mtaraji kufanikiwa. (*Tazama Maelezo 3:200*).

Sura 4 - An-Nisaa

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

1. Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni.¹
2. Na wapeni mayatima mali yao. Wala msibadilishe kibaya kwa kizuri. Wala msile mali zao pamoja na mali zenu. Hakika yote hayo ni jukumu kubwa.²
3. Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtowafanyia mayatima uadilifu, basi oeni mnao wapenda katika wanawake, wawili au watatu au wane. na mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi mmoja tu, au wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki. Kufanya hivi ndiko kutapelekea msikithirishie wana.³
4. Na wapeni wanawake mahari yao hali ya kuwa ni kipawa. Lakini wakikutunukieni kitu katika mahari, kwa radhi yao, basi kileni kiwashuke kwa raha.⁴
5. Wala msiwape wasio na akili mali yenu ambayo Mwenyezi Mungu ameyajaalia yawe ni kiamu yenu. Walisheni katika hayo na muwavike, na msemi nao maneno mazuri.⁵
6. Na wajaribuni mayatima mpaka wafike umri wa kuo. Mkiwaona ni wekevu, basi wapeni mali yao. Wala msiyale kwa fujo na pupa kwa kuwa watakuja kuwa watu

1 Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na kutokana na nafsi hiyo akamuumba mkewe, na kutokana na hao wawili, wakaenea wanaume na wanawake wengi. Basi nyote mnatokana na nafsi moja. Mcheni Mwenyezi Mungu mnaye mtaka msaada kwa kila mnacho kihitajia, na kwa jina lake ndio mnaombana nyinyi kwa nyinyi katika mambo yenu. Pia tahadharini na kuacha kuwasaidia jamaa zenu, wa karibu na wa mbali. Kwani Mwenyezi Mungu daima anakuangalieni. Hapana chochote katika mambo yenu kinacho fichikana kwake. Na Yeye ndiye Mwenye kukulipeni.

2 Na wapeni mayatima mali yao wanayo stahiki, na yalindeni mali yao vizuri, wala msiwape kilio duni mkawanyima kizuri. Wala msichukue mali yao mkaongezea kwenye mali yenu. Hakika kitendo hicho ni dhambi kubwa.

3 Ilivyo kuwa mnakhofu kuwadhulumu mayatima kwa kuwa hiyo ni dhambi kubwa, basi kadhaalika khofuni machungu ya wake zenu kwa kuacha kuwafanyia uadilifu baina yao, na kuzidisha juu ya wane. Basi mnaweza kuo wawili, au watatu, au wane, ikiwa mna imani kuwa mtaweza kufanya uadilifu. Mkiogopa kuwa hamtaweza kufanya uadilifu basi oeni mmoja tu, au jitoshelezeni na wajakazi walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Hayo ni afadhali kuliko kwenda kuingia katika dhulma na ujeuri. Na ni afadhali msije mkawa na watoto wengi bila ya kiasi hata mshindwe kuwatazama. (Wafasiri wengi wamependelea kufasiri “Alla Tau’luu” kuwa “Kutofanya jeuri au dhulma.” Lakini hii AL MUNTAKHAB imekhiari tafsiri hii ya “msikithirishie wana”, ambayo ndiyo aliyo ifuata Imam Shaafii r.a., naye alitanguliwa na Maimamu wanazuoni wa Kiislamu, Zayd bin Aslam r.a. na Jabir bin Zayd r.a. kama alivyo simulia Daar Qut’ni, na imetajwa katika Tafsir ya Qurt’uby juzuu ya 5 sahifa 22.) (Tazama Maelezo 4:3)

4 Wapeni wanawake mahari yao kuwa ni kipawa, tunza iliyo safi. Na nyinyi hamna haki yoyote katika hayo mahari. Ikiwa hao wanawake kwa radhi ya nafsi zao wenyewe wakakubali kusamehe sehemu yoyote ya mahari mliyo kwisha ahadiana, basi hapo mnayo ruhusa kuchukua na mkatumia kwa kheri na salama.

5 Wala msiwape wasio na akili ya kutosha kuendesha mambo yao mali yao, nayo ni mali yenu vile vile. Kwani mali ya yatima na ya mchache wa akili yamekulazimuni myatazame yasiharibike. Mwenyezi Mungu ameyajaalia mali hayo ya kukimu maisha. Wapeni kutokana na pato lake sehemu kama wanavyo hitajia kwa kula, na wavisheni na muwatendee vyema, na msemi nao maneno ya kuwaridhisha sio ya kuwaudhi au kuwadhili.

wazima. Na aliye kuwa tajiri naajizuilie, na aliye fakiri basi naale kwa kadri ya ada. Na mtakapo wapa mali yao washuhudizieni. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Mhasibu.⁶

7. Wanaume wana sehemu katika wanayo yaacha wazazi na jamaa walio karibia. Na wanawake wanayo sehemu katika waliyo yaacha wazazi na jamaa walio karibia. Ikiwa kidogo au kingi. Hizi ni sehemu zilizo faridhiwa.⁷

8. Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na masikini, wapeni katika hayo mali ya urithi, na semeni nao maneno mema.⁸

9. Na wachelee wale ambao lau kuwa na wao wangeli acha nyuma yao watoto wanyonge wangeli wakhofia. Basi nao wamche Mwenyezi Mungu, na waseme maneno yaliyo sawa.⁹

10. Hakika wanao kula mali ya mayatima kwa dhulma, hapana shaka yoyote wanakula matumboni mwao moto, na wataingia Motoni.¹⁰

11. Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili. Na ikiwa wanawake zaidi ya wawili, basi watapata thuluthi mbili za alichio kiacha maiti. Lakini akiwa mtoto mwanamke ni mmoja, basi fungu lake ni nusu. Na wazazi wake wawili, kila mmoja wao apate sudusi ya alichio kiacha, ikiwa anaye mtoto. Akiwa hana mtoto, na wazazi wake wawili wamekuwa ndio warithi wake, basi mama yake atapata thuluthi moja. Na akiwa anao ndugu, basi mama yake atapata sudusi. Haya ni baada ya kutolewa alichio usia au kulipa deni. Baba zenu na watoto wenu, nyinyi hamjui ni nani baina yao aliye karibia zaidi kwenu kwa manufaa. Hiyo ni Sharia iliyo toka kwa Mwenyezi Mungu. Bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima.¹¹

6 Na kabla ya hao mayatima kufika umri wa kubaalighi wajaribuni, mpate kujua akili zao na hali zao na maarifa yao katika kuendesha mambo. Hata wakifika wakati wa kusilihi kuoa na mkauona uwekevu wao, na matayarisho kuchukua jukumu, basi hapo wapeni mali yao wenyewe. Wala nyinyi msiyale mali yao kwa fujo, mkifanya haraka mpatilize kabla hawajabaalighi wakawa watu wazima ikabidi haki yao kurudi. Na akiwa katika mawasii anajitoshia kwa utajiri, basi ajizuie asichukue chochote kuwa ni ujira kutazama mali ya mayatima. Na akiwa fakiri muhitaji basi ajitosheleze kuchukua ujira wa uangalizi kwa kadri ya ada ilivyo. Na mnapo wakabidhi mayatima mali yao wekeni mashahidi wa kushuhudia. Na mjue kuwa Mwenyezi Mungu daima yupo nyuma yenu, na Yeye ndiye Mhasibu, na Yeye ndiye Muangalizi. Na Yeye anatosha kuwa Mhasibu na Muangalizi.

7 Wanaume wanalo fungu lao katika mali waliyo yaacha kurithiwa wazazi wawili na jamaa walio karibia. Na wanawake, aidha, wana fungu lao, bila ya kunyimwa au kupunjwa. Na mafungu hayo yamethibiti, na yamefaridhiwa, na yamekadiriwa, yakiwa mali yenyewe kidogo au mengi.

8 Na pindi ikiwa wamehudhuria wakati ule wa kugawanya urithi baadhi ya jamaa ambao hawarithi, na ni mayatima na masikini, basi wakirimuni kwa kuwapa chochote katika huo urithi ili kuzipoza nafsi zao, na kuondoa uhasidi katika nyoyo zao. Na ni vizuri pia katika kuwapa kuleta maneno laini na udhuru mwema.

9 Watu watahadhari na kuwadhulumu mayatima, na wawaogopee watoto wao wanyonge wasije na wao wakadhulumiwa kwa watendavyo wazee kwa mayatima wa watu wengine. Na wamwogope Mwenyezi Mungu katika kuwatendea mayatima. Na waseme maneno yaliyo kaa sawa yanayo fuata haki, wala wasimdhulumu yeyote.

10 Hakika wanao wadhulumu mayatima kwa kuchukua mali yao bila ya haki, hakika wanakula yatakayo wapelekea Motoni. Na Mwenyezi Mungu atawaadhibu Siku ya Kiyama kwa moto mkali wenye kutia machungu. (Je, huwaje basi adhabu ya mwenye kudhulumu mali ya Mwenyezi Mungu? Wakfu za misikiti, madrasa n.k.? Na huwaje mwenye kuuwa ili apate kudhulumu mali ya mayatima wa hao alio wauwa?)

11 Mwenyezi Mungu anakuamrisha katika mambo ya kuwarithisha watoto wenu na wazazi wenu, pindi mtakapo kufa, kwa njia inayo leta uadilifu na maslahi. Nayo ni kuwa sehemu ya mwanamume ni sawa

12. Na fungu lenu ni nusu walicho acha wake zenu ikiwa hawana mtoto. Wakiwa na mtoto basi fungu lenu ni robo ya walicho acha, baada ya wasia waliyo usia au kulipa deni. Na wake zenu watapata robo mlichio kiacha, ikiwa hamna mtoto. Mkiwa mna mtoto basi sehemu yao ni thumni ya mlichio kiacha, baada ya wasia mlio usia au kulipa deni. Na ikiwa mwanamume au mwanamke anaye rithiwa hana mtoto wala wazazi, lakini anaye ndugu mume au ndugu mke, basi kila mmoja katika hawa atapata sudusi. Na wakiwa zaidi kuliko hivyo basi watashirikiana katika thuluthi, baada ya wasia ulio usiwa au kulipa deni, pasio kuleta dhara. Huu ndio wasia ulio toka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mpole.¹²

13. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anaye mt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Yeye atamtia katika Pepo zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.¹³

14. Na anaye muasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akaipindukia mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) atamtia Motoni adumu humo, na atapata adhabu ya kudhalilisha.¹⁴

15. Na ambao wanafanya uchafu miongoni mwa wanawake wenu, washuhudizieni

na sehemu ya wanawake wawili, ikiwa watoto wanao rithi ni wanaume na wanawake. Ikiwa watoto wote ni wanawake watupu, na idadi yao imezidi wawili, basi sehemu yao ni thuluthi mbili za tirka, yaani mali yaliyo achwa na maiti. Inafahamika katika madhumuni ya Aya kuwa fungu la binti wawili ni kama fungu la walio zidi hapo. Na akiwa mtu amemuacha binti mmoja tu, basi fungu lake ni nusu ya alichio kiacha. Na akiwa mtu amemuacha baba na mama, basi kila mmojapo kati ya hao atapata sudusi, yaani sehemu moja katika sita, ikiwa huyo maiti alikuwa na mtoto mmoja - mwanamume au mwanamke - pamoja na hao wazazi wake. Akiwa hana mtoto na wakamrithi wazazi wake tu, basi mama sehemu yake ni thuluthi, na kilicho baki ni cha baba. Na ikiwa huyo maiti alikuwa na ndugu, basi mama yake atapata sudusi na kilicho baki ni cha baba, na wale ndugu hawapati chochote. Mafungu hayo hupewa wanao stahiki baada ya kwisha lipwa deni lilio kuwa juu ya maiti, na kutimiza yale aliyo yausia katika mipaka aliyo ruhusu Mwenyezi Mungu. Hii ni hukumu ya Mwenyezi Mungu. Na huu ndio uadilifu na ndio hikima. Na nyinyi hamjui ni nani kwenu mwenye manufaa zaidi kwenu, baina ya wazazi na wana. Na kheri khasa ni aliyo yaamrisha Mwenyezi Mungu, kwani Yeye ndiye Mwenye kuyajua maslahu yenu, na ndiye Mwenye hikima katika yale aliyo kulazimisheni.

12 Fungu la mume ni nusu ya alichio acha mke ikiwa huyo mke hakuacha mtoto kutokana na mume huyo au mwengine. Akiwa huyo mke ana mtoto, basi mumewe atapata robo baada ya kutolewa wasia aliye usia huyo mwanamke au kulipwa deni lake. Na fungu la mke au wake ni robo ya alichio acha mume ikiwa hakuacha mtoto kwa wake hao au wengine. Akiwa anaye mwana kutokana na hao au wake wengine basi mke huyu au wake hawa watapata thumni ya tirka baada ya wasia alio usia au deni. Na mwana wa mwana, yaani mjukuu, ni kama mwana katika haya yaliyo tangulia. Na akiwa maiti ni mwanamume au mwanamke, naye hana mwana wala mzazi, na kamwacha ndugu mume kwa mama, au ndugu wawili wa kike kwa mama, basi kila mmoja wao atapata sudusi, yaani sehemu moja katika sita. Na wakiwa wengi kuliko hivyo watashirikiana katika thuluthi, watagawana sawa sawa wanaume na wanawake kwa mujibu wa ushirika, baada ya kulipa madeni yaliyo kuwa juu yake, na kutimiza wasia ambao haudhuru urithi, nao ni wasia usio pindukia thuluthi iliyi baki baada ya kulipa madeni. Basi, enyi Waumini! Jilazimisheni kufuata aliyo kuusieni Mwenyezi Mungu; kwani Yeye hakika ni Mwenye kujua vyema nani miongoni mwenu anaye dhulumu na nani anaye fanya uadilifu, Yeye ni Mpole hafanyi haraka kutoa adhabu.

13 Hizo ni hukumu zilizo tajwa kueleza khabari ya mirathi na mengine yaliyo tangulia ni Sharia za Mwenyezi Mungu aliye zipanga kwa ajili ya waja wake wazijue wala wasizikiuke. Na Mwenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika alivyo hukumu Yeye malipwa yake yatakuwa ni Pepo ipitayo mito kati yake, na atakaa humo daima dawamu. Na huko ndiko kushinda kukubwa. (*Tazama Maelezo 4:13*)

14 Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake na akaikiuka mipaka aliyo iweka Mwenyezi Mungu, na huku akihalalisha kukiuka huko basi mtu huyo atalipwa Moto, na humo atakaa milele, akiadhibiwa mwili wake juu ya kuadhibiwa roho yake.

watu wane katika nyinyi. Watakapo shuhudia, basi wazuieni majumbani mpaka wafishwe na mauti au Mwenyezi Mungu awatolee njia nyengine.¹⁵

16. Na wawili kati yenu wafanyao hayo waadhibuni. Na wakitubia wakatengenea basi waacheni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kupokea toba, Mwenye kurehemu.¹⁶

17. Hakika toba inayo kubaliwa na Mwenyezi Mungu ni ya wale wafanyao uovu kwa ujinga, kisha wakatubia kwa haraka. Hao ndio Mwenyezi Mungu huwakubalia toba yao, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na ni Mwenye hikima.¹⁷

18. Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yakamfikia mmoja wao mauti, kisha hapo akasema: Hakika mimi sasa nimetubia. Wala wale wanao kufa na hali wao ni makafiri. Hao tumewaandalia adhabu chungu.¹⁸

19. Enyi mlio amini! Si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu. Wala msiwadhikishe ili mwapokonye baadhi ya mliyvo wapa - isipo kuwa wakifanya uchafu ulio wazi. Na kaeni nao kwa wema, na ikiwa mmewachukia, basi huenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake.¹⁹

20. Na mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke, na hali mmoja wao mmempa chungu ya mali, basi msichukue katika hayo kitu chochote. Je, mtachukua kwa dhulma na kosa lilio wazi?²⁰

15 Na wale wanawake wanao zini wakishuhudiwa na mashahidi wanaume wane walio waadilifu, basi wazuieni wasitoke nyumbani kwa ajili ya kuwalinda na kuzuia usiendelee ufisadi na shari mpaka wafe, au Mwenyezi Mungu awafungulie njia ya maisha yaliyo sawa kwa kuolewa na kutubu. (Wafasiri wengine wanasema hukumu hii ni kwa wanawake wanao fanya mambo machafu wenyewe kwa wenyewe, sio ya zina baina ya mwanamke na mwanamume. Kwa kuhifadhi heshima ya wanawake inalazimu wapatikane mashahidi wane, badala ya wawili, walio ona kitendo khasa, sio kuwatuhumu watu kwa jambo ova kama hilo bila ya mashahidi wane walio shuhudia kwa macho yao.)

16 Mwanamume na mwanamke walio zini, nao hawajaoa (au kuolewa), wapewe adhabu maalumu, pindi ikithibiti hiyo zina kwa mashahidi wane waadilifu. Wakitubu baada ya kupewa adhabu, basi msiwatajje hayo maasi waliyo yatenda, wala msiwaaziri. Hakika Mwenyezi Mungu kwa rehema yake anakubali toba ya wenyewe kutubu.

17 Hakika toba imedhaminiwa na Mwenyezi Mungu kwa watendao maovu katika hali ya ujinga, na kupitikiwa na kutoangalia vyema, kisha wakafanya haraka ya kutubu kabla ya kufikiwa na mauti. Hawa basi Mwenyezi Mungu anaikubali toba yao, naye ni Mjuzi, haumfichikii ukweli wa toba, ni Mwenye hikima, hakosei katika kupima.

18 Toba isiyo kubaliwa ni ya wanao fanya maasi kisha hawafanyi haraka kuyajutia mpaka mmoja afikwapo na mauti. Tena hapo husema: Sasa mimi natangaza majuto na toba. Kadhaalika toba haikubaliwi kutokana na wanao kufa katika ukafiri. Mwenyezi Mungu ameyaandalia makundi mawili hayo adhabu ya kutia uchungu huko kwenye nyumba ya malipo, Akhera.

19 Enyi mlio amini! Haikujuziini kuwafanya wanawake kama bidhaa, mkiwarithi wake zenu bila ya mahari na bila ya ridhaa yao. Wala msiwadhulumu kwa kuwadhikisha ili wapate kusamehe baadhi ya mahari mlio wapa. Wala msiwadhiki ili wapate kukurejesheni mali mlio wapa, ila ikiwa wakifanya kosa wazi la kuwacha ut'iifu, au la tabia mbovu, au la ukahaba. Hapo mnaweza kuwadhikisha au kuchukua baadhi ya mlicho wapa wakati wa kufarikiana nao. Na ni waajibu wenu, enyi Waumini, kukaa na wake zenu kwa vizuri, kwa maneno mema na vitendo vyema. Ikiwa mtawachukia kwa aibu fulani katika tabia au katika umbo au mengineyo, basi juu ya hivyo subirini. Msifanye haraka kuwacha, kwani asaa Mwenyezi Mungu akajaalia kheri nyingi katika hicho hicho mkichukiacho. Na ujuzi wa mambo yote uko kwa Mwenyezi Mungu tu.

20 Na pindi ikiwa mnataka kubadili mke pahala pa mke mwengine, na ikawa mmempa mmoja wao mali mengi basi si halali kwenu kuchukua chochote katika hayo. Jee mtachukua hayo kwa njia ya upotovu na kwa dhambi iliyo wazi?

- 21.** Na mtachukuaje na ilhali mmekwisha ingiliana nyinyi kwa nyinyi, na wao wanawake wamechukua kwenu ahadi iliyo madhubuti?²¹
- 22.** Wala msiwaoe wake walio waoa baba zenu, ila yaliyo kwisha pita. Hakika huo ni uchafu na uchukizo na ni njia mbaya.²²
- 23.** Mmeharimishiwa mama zenu, na binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na khaalati zenu, na binti wa ndugu mume, na binti wa dada, na mama zenu walio kunyonyesheni, na dada zenu kwa kunyonya, na mama wa wake zenu, na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu walio zaliwa na wake zenu mlio waingilia. Ikiwa hamkuwaingilia basi hapana lawama juu yenu. (Pia mmeharimishwa) wake wa watoto wenu walio toka katika migongo yenu. Na kuwaoa pamoja dada wawili isipo kuwa yale yaliyo kwisha pita. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.²³
- 24.** NA WANAWAKE wenye waume, isipo kuwa walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Ndiyo Sharia ya Mwenyezi Mungu juu yenu. Na mmehalilishiwa wasio kuwa hao, mtafute kwa mali yenu kwa kuowa pasina kuzini. Kama mnavyo starehe nao, basi wapeni mahari yao kwa kuwa ni waajibu. Wala hapana lawama juu yenu kwa mtakacho kubaliana baada ya kutimiza waajibu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua na Mwenye hikima.²⁴
- 25.** Na asiyeweza kati yenu kupata mali ya kuolea wanawake wa kiungwana Waumini, na aoe katika vijakazi Waumini iliyo wamiliki mikono yenu ya kulia. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa imani yenu. Nyinyi mmetokana wenyewe kwa wenyewe. Basi waoeni kwa idhini ya watu wao, na wapeni mahari yao kama ada, wawe wanawake wema, si makahaba wala si mahawara. Na wanapo olewa kisha wakafanya uchafu basi adhabu yao itakuwa ni nusu ya adhabu waliyo wekewa waungwana. Hayo ni kwa yule miongoni mwenu anaye ogopa kuingia katika zina. Na mkisubiri ndio bora kwenu. Na

21 Na vipi ikufalieni nyinyi kutaka kurudishiwa mahari mliyo kwisha yatoa, na hali mlukwisha changanyika nyinyi kwa nyinyi, na wao wanawake wakafungamana nanyi kwa agano lenye nguvu ambalo kwalo Mwenyezi Mungu amewajibisha muingiane nao kwa ndoa.

22 Wala nyinyi, watoto, msiwaoe wanawake walio wahi kuolewa na baba zenu. Jambo hilo ni uchafu na linachusha, na linakirihwa na Mwenyezi Mungu na watu. Na hiyo ni njia ovu kabisa. Lakini Mwenyezi Mungu anasamehe yaliyo kwisha tendeka katika zama za ujahili. (Tazama Maelezo 4:22)

23 Mwenyezi Mungu amekuharimishieni kuwaoa mama zenu, na binti zenu, na dada zenu (ndugu wanawake) na shangazi zenu, na khaalati zenu (mama wadogo) na binti wa ndugu, na binti wa dada, na mama walio kunyonyesheni, na dada zenu kwa kunyonya, na mama wakwe. Na walio harimishwa bila ya kunasibiana kwa damu ni: mama wa kunyonyesha, dada wa kunyonya, mama mkwe, binti za wake kwa waume wengine ikiwa hao wake wameingiliwa, na wake wa watoto mlio wazaa, na kuwaoa pamoja ndugu wawili. Yaliyo pita katika siku za ujahili yamesamehewa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe kwa yaliyo pita kabla ya mpango huu, na Mwenye kuwarehemu katika aliyo kuwekeeni sharia. (Tazama Maelezo 4:23)

24 Haramu kwenu kuoa wake za watu wote, waungwana na wasio waungwana, ila mateka mlio wateka katika vita baina yenu na makafiri. Kwani ndoa zao zilizo pita zinafutika kwa kutekwa. Wanakuwa halali kwenu baada ya kuhakikisha hawana mimba. Basi shikeni aliyo kuandikieni Mwenyezi Mungu kuhishimu mlicho katazwa. Isipo kuwa hao wanawake Waumini walio maharimu yenu, mwaweza kutafuta wanawake mkawaoa kwa mali yenu, bila ya kuzini au kuweka kinyumba. Kila mwanamke mliye starehe naye baada ya kumwoa mpeni mahari yake kama mliyoye patana. Hapana ubaya kwenu ikiwa watakuridhieni kupunguza au kuongeza. Mwenyezi Mungu daima anayaangalia mambo ya waja wake, na ni mwenye kuwapangia hukumu zinazo wasilili kwa maisha yao

Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.²⁵

26. Mwenyezi Mungu anataka kukubainishieni na kukuongozeni nyendo za walio kuwa kabla yenu, na akurejezeni kwenye ut'iifu wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hikima.²⁶

27. Na Mwenyezi Mungu anataka kukurejezeni kwenye ut'iifu wake, na wanao taka kufuata matamano wanataka mkengeuke makengeuko makubwa.²⁷

28. Mwenyezi Mungu anataka kukupunguzieni taabu, na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.²⁸

29. Enyi mlio amini! Msiliane mali yenu kwa dhulma, isipo kuwa iwe biashara kwa kuridhiana wenyewe. Wala msijiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwarehemuni.²⁹

30. Na mwenye kutenda hayo kwa uadui na udhaalimu, basi huyo tutamwingiza Motoni. Na hilo ni jepesi kwa Mwenyezi Mungu.³⁰

31. Mkiyaepuka makubwa mnayo katazwa, tutakufutieni makosa yenu madogo, na tutakuingizeni mahali patukufu.³¹

32. Wala msitamani alichu wafadhili Mwenyezi Mungu baadhi yenu kuliko wengine. Wanaume wana fungu katika walio vichuma, na wanawake wana fungu katika walio vichuma. Na muombeni Mwenyezi Mungu fadhila zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.³²

25 Asiye weza kati yenu kuwaoa wanawake Waumini wa kiungwana basi na aowe anaye muweza katika wanawake Waumini walio milikiwa. Na Mwenyezi Mungu anajua vyema ukweli wa Imani yenu na ikhlasi yenu. Wala msione uvunjifu kuwaoa hao vijakazi, kwani nyinyi na wao ni sawa katika Dini. Basi waoweni kwa idhini ya watu wao, na muwape mahari yao mliyo wakadiria kwa mujibu ya ilivyo zowewa kati yenu kwa ajili ya kutendana mema na kutimiza haki. Na chagueni wanawake walio safi, msichague wazinifu kwa dhaahiri wala mahawara wa kinyumba. Na hao wakija zini baada ya kuolewa basi adabu yao ni nusu ya muungwana. Na huku kuhalalishiwa kuowa wajakazi mnapo kuwa hamuwezi kunajuzu kwa anaye ogopa taabu zinazo pelekea zina. Na mkisubiri kuto owa wajakazi na mkakaa safi ni bora kwenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, na Mkubwa wa kurehemu.

26 Mwenyezi Mungu anataka kukuwekeeni wazi njia yenye maslaha kabisa, na akuongoeni kwenye nyendo njema za walio kuwa kabla yenu, na akurejesheni kwenye njia ya ut'iifu wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua vyema mambo yenu, ni Mwenye kupanga baraabara katika hukumu zake kwa yanayo silihi mambo yenu.

27 Na Mwenyezi Mungu anataka mrejee katika ut'iifu wake, na wale wanao fuata ladha zao, na matamano yao machafu, miongoni mwa makafiri na waasi, wanataka muwe mbali kabisa na njia ya haki.

28 Mwenyezi Mungu anataka kukufanyieni wepesi katika kutunga sharia ambazo ndani yake zina sahala na takhifu kwenu. Kwani hakika Mwenyezi Mungu amemuumba mwanaadamu kiumbe dhaifu katika kupambana na matamano na maelekeo ya nafsi. Kwa hivyo yanayo mlazimu katika sharia yana wepesi na wasaa. Na hayo kwa fadhila yake na taisiri yake Mwenyezi Mungu ndiyo anayo walazimisha waja wake.

29 Enyi mlio amini! Msinyang'anyane mali nyinyi kwa nyinyi. Lakini ipo ruhusa kufanya biashara kwa kuridhiana. Wala msijiteketeze kwa kuacha amri za Mola wenu Mlezi. Wala mmoja wenu asimtende uwovu mwenziwe, kwani nyote ni nafsi moja. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye rehema daima kwenu.

30 Na mwenye kuyatenda aliyo yaharimisha Mwenyezi Mungu kwa uvamizi na kupindukia haki yake, basi tutamtia Motoni ateketee huko. Na hayo ni madogo na mepesi kabisa kwa Mwenyezi Mungu.

31 Mkiyaachilia mbali madhambi makubwa makubwa anayo kukatazeni Mwenyezi Mungu, tutakusameheni makosa yaliyo duni ya hayo, maadamu mnafanya ukomo wa juhudi yenu kwenda sawa; na tutakuwekeni duniani na Akhera mwahali penye ihsani na hishima kwenu.

32 Wala haifai wanaume kutamani yale waliyo khusishwa nayo wanawake, wala haiwafalii wanawake kutamani waliyo khusishwa nayo wanaume. Kwani kila kikundi kina sehemu yake kwa mujibu wa tabia

33. Na kila mmoja tumemwekea warithi katika waliyo yaacha wazazi wawili na jamaa. Na mlio fungamana nao ahadi wapeni fungu lao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kila kitu.³³

34. Wanaume ni wasimamizi wa wanawake, kwa kufadhiliwa na Mwenyezi Mungu baadhi yao juu ya baadhi, na kwa mali yao wanayo yatoa. Basi wanawake wema ni wale wenye kut'i ni na wanao jilinda hata katika siri kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameamrisha wajilinde. Na ambao mnachelea kutoka katika ut'iifu wanasihini, muwahame katika malazi na wapigeni. Wakikut'iini msiwatafutie njia ya kuwaudhi bure. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliye juu na Mkuu.³⁴

35. Na mkichelea kutakuwapo mfarakano baina ya mke na mume basi pelekeni muamuzi kutokana na jamaa za mume, na muamuzi kutokana na jamaa za mke. Wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye khabari.³⁵

36. Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wanao jifakhiri,³⁶

37. Ambao wanafanya ubakhili na wanaamrisha watu ubakhili, na wanaficha fadhila

ya maumbile ya kazi zinazo wawajibikia, na haki wanazo ongezewa. Basi kila mmoja ajielekeze kutaraji ziada ya fadhila za Mwenyezi Mungu kwa kukuza vipawa alivyo pewa yeye na kutafuta msaada juu ya wajibu ulio juu yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi timamu wa kila kitu, na mtu amepewa namna ya kila kitu kinacho msilihi.

33 Na wote, wanaume na wanawake, tumewajaalia kuwa wanastahiki urithi wao wa kuwarithi wazazi wawili, na jamaa, na wale ambao mfiliwa amefungamana nao kwa agano ambalo matokeo yake ni kuwa amrithi ijapokuwa si jamaa, na amsaidie pindi anahitajia msaada kuwa ni badala yake. Basi mpeni haki yake kila mwenye haki, wala msipunguze kitu. Hakika Mwenyezi Mungu anakuangalieni kwa kila kitu, na yuko pamoja nanyi, anashuhudia yote myafanyayo.

34 Wanaume wana haki ya kuwaangalia na kuwachunga wanawake, na kuwasimamia katika mambo yao kwa vile Mwenyezi Mungu amewapa wao wanaume sifa za kuweza kuisimamia haki hii, na kwa kuwa wao ndio wanao hangaika na kufanya juhudi ya kutafuta mali ya kuutumilia ukoo mzima. Basi wanawake wema wanakuwa ni wat'iifu kwa Mwenyezi Mungu na waume zao. Ni wenye kuhifadhi vyote ambavyo waume zao hawavioni kwa sababu Mwenyezi Mungu ameamrisha vihifadhiwe, na kwa kuwapa wao tawfiki. Na wanawake wanao onyesha kuanza uasi wanasihini kwa maneno yenye kuathiri. Kama hawakusikia tenganeni nao kitandani. Hawakusikia, watieni adabu kwa pigo dogo, si la kuwajuruhi wala kuwadhalilisha. Wakirejea kwenye ut'iifu wenu kwa njia mojawapo katika hizi tatu basi msiwatafutie kisababu cha kuwatesa zaidi kuliko haya. Hakika Mwenyezi Mungu yuko juu yenu, naye atakupatilizeni pindi mkiwaudhi wake zenu au mkawafanyia jeuri.

35 Pindi pakitokea kukhitalifiana baina ya mke na mume, na mkakhofia kutokea kufarikiana kutako leta t'alaka, chagueni waamuzi wawili. Mmoja kutokana na upande wa mume na mwengine upande wa mke. Wakitaka kusuluhiana Mwenyezi Mungu atawawafikisha wafikilie lilio kheri kwa wote wawili, nako ama kukaa kwa wema au kuachana kwa ihsani. Hakika Mwenyezi Mungu anachungua kila kitu cha waja wake, kilicho dhihiri na kilicho fichikana.

36 Nanyi muabuduni Mwenyezi Mungu peke yake, wala msimfanyie washirika katika Ungu na kuabudiwa. Na watendeeni wema wazazi wenu bila ya taksiri yoyote, na pia jamaa zenu, na mayatima, na walio fakirika kwa sababu ya kuemewa au kupata masaibu katika mali yao, na jirani mliye karibiana naye kwa nasaba, na jirani mtu mbali, na mwenzio katika kazi au njia au majlisi, na msafiri mhitaji asiye kuwa na kituo katika nchi maalumu, na watumwa wenu wanaume na wanawake mlio wamiliki. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi anaye jipa ubora juu ya watu wengine, na hawachukulii watu kwa huruma, na anakithirisha kujisifu mwenyewe kwa kujifakhiri.

alizo wapa Mwenyezi Mungu. Na tumewaandalia makafiri adhabu ya fedheha,³⁷

38. Na ambao hutoa mali yao kwa kuonyesha watu, wala hawamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho; na yule ambaye Shet'ani amekuwa ndiye rafiki yake, basi ana rafiki mbaya mno.³⁸

39. Na ingeli wadhuru nini wao lau wangeli muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wakatoa katika aliyo waruzuku Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwajua vyema.³⁹

40. Hakika Mwenyezi Mungu hadhulumu hata uzito wa chembe moja. Na ikiwa ni jambo jema basi Yeye hulizidisha na hutoa kutoka kwake malipo makubwa.⁴⁰

41. Basi itakuwaje pindi tukiwaletea kutoka kila umma shahidi, na tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?⁴¹

42. Siku hiyo walio kufuru na wakamuasi Mtume watatamani ardhi isawazishwe juu yao. Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote.⁴²

43. Enyi mlio amini! Msikaribie Sala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayo yasema, wala hali mna janaba - isipo kuwa mmo safarini - mpaka mkoge. Na mkiwa wagonjwa, au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni, au mmewagusa wanawake - na msipate maji, basi ukusudieni mchanga safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye kughufiria.⁴³

44. Huwaoni wale walio pewa sehemu ya Kitabu wananunua upotovu na wanakutakeni

37 Hao ndio wanao ongeza juu ya takaburi na tafakhuri yao ila ya kuwafanyia watu ubakhili kwa mali yao na juhudi yao. Tena ikawa wanawataka watu wafanye ubakhili kama wao. Kazi yao ni kukhofia neema na fadhila ya Mwenyezi Mungu isiwatoke. Kwa hivyo, basi, hawajifai wenyewe wala hawawafai watu. Wapinzani kama hao tumekwisha waandalia adhabu ya kutia machungu na ya kudhalilisha.

38 Na Mwenyezi Mungu hawapendi wanao toa mali kwa ajili ya kuonekana na watu, wapate kuwasifu na kuwatukuza, na ilhali wao si wenye kumuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Malipo. Kwani hao wamemfuata Shetani naye amewapoteza. Na mwenye kuwa rafiki yake ni Shetani basi ana rafiki mbaya kweli.

39 Ama wamelaanika watu hawa! Kingewadhuru nini wao lau kuwa wamemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Akhera, na wakatoa katika alichu wapa Mwenyezi Mungu kwa kufuatana na Imani hii, na usafi wa niya, na kutaraji thawabu kama ilivyo wajibikia? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kwa ujuzi kaamili mambo yote yaliyo wazi na yaliyo fichikana ndani.

40 Hakika Mwenyezi Mungu hamdhulumu mtu hata kidogo. Basi hampunguzii ujira wake mtu, wala adhabu yake hamzidishii kabisa. Bali humzidishia mtenda mema thawabu zake mardufu hata zikiwa kidogo vipi. Na humpa kwa fadhila yake malipo makubwa yasiyo lingana na hayo mema yake ambayo yamekwisha zidishwa mardufu.

41 Vipi basi itakuwa hali ya hao mabakhili wanao pingana na aliyo yaamrisha Mwenyezi Mungu, tutapo mleta Siku ya Kiyama kila Nabii awe ni shahidi juu ya kaumu yake, na tukakuleta wewe, ewe Nabii Muhammad, kuwa ni shahidi juu ya kaumu yako, na hali miongoni mwao wapo hao wanao zuia mali yao na wanao pinga?

42 Yatapo tokea haya watatamani hao wapinzani wanao pinga lau kuwa wangeli potea chini ya ardhi kama wanavyo potea maiti makaburini! Na wao hawawezi kumficha Mwenyezi Mungu kitu chochote katika mambo yao, na hali zao na vitendo vyao vitadhihiri.

43 Enyi mlioamini! Msende kusali misikitini nanyi mmo katika hali ya ulevi mpaka muwe mnafahamu myasemayo. Wala msiingie misikitini nanyi mna janaba, ila ikiwa ni kupita njia tu bila ya kusita, mpaka mtahirike kwa kukoga. Na mkiwa ni wagonjwa hamuwezi kutumia maji kwa kuogopa maradhi yasikuzidini au kuchelewa kupona, au mkiwa mmo safarini na ipo shida ya kupata maji, basi tumieni mchanga ulio safi. Kadhaalika mmoja wenu akitoka chooni, au mkawaingilia wanawake na mkawa hamkupata maji ya kujitahirishia kwa kukosekana kwake, basi vile vile chukueni mchanga safi upigeni kwa mikono yenu, na mpangusie nyuso zenu na mikono yenu. Hakika ni shani ya Mwenyezi Mungu kuwa ni Mwenye kusamehe sana na Mwenye kufuta dhambi.

nanyi mpootee njia?⁴⁴

45. Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema maadui zenu. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa ni Mlinzi, na anatosha kuwa ni Mwenye kukunusuruni.⁴⁵

46. Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahala pake, na husema: Tumesikia na tumeasi, na sikia bila ya kusikilizwa. Na husema: “Raai’naa”, kwa kuzipotoa ndimi zao ili kuitukana Dini. Na lau kama wangeliki sema: Tumesikia na tumet’ii, na usikie na “Undhurna” (Utuangalie), ingeli kuwa ni kheri kwao na sawa zaidi. Lakini Mwenyezi Mungu amewalaani kwa kufuru yao; basi hawaamini ila wachache tu.⁴⁶

47. Enyi mlio pewa Kitabu! Aminini tuliyo yateremsha yenye kusadikisha yale mliyo nayo, kabla hatujazigeuza nyuso tukazipeleka kisogoni, au tukawalaani kama tulivyo walaani watu wa Sabato (Jumaamosi). Na amri ya Mwenyezi Mungu ni lazima ifanyike.⁴⁷

48. Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi hakika amezua dhambi kubwa.⁴⁸

49. Jee huwaoni wale wanao dai kuwa ati wametakasika? Bali Mwenyezi Mungu humtakasa amtakaye. Na hawatadhulumiwa hata kadiri ya kijiuzi kilichomo ndani ya uwazi wa kokwa ya tende.⁴⁹

44 Hebu huyastaajabii mambo ya hawa walio pewa sehemu ya Vitabu vilivyo tangulia wanavyo acha uwongofu na wakatafuta upotovu katika mambo yaliyo wakhusu nafsi zao! Na wao tena wanakutakeni nyinyi mjitenge na Haki ambayo ndiyo Njia ya Mwenyezi Mungu Iliyo Nyooka!

45 Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi kuliko nyinyi kuwajua maadui zenu wa kweli, na anatambua zaidi yaliyo ndani ya nafsi zao. Ulinzi wa Mwenyezi Mungu unakulindeni, na unakuangalieni, na unakutosheni. Basi msitafute ulinzi wa mwenginewe usio kuwa wake. Msaada na nusura yake inakutoshelezeni; basi msiwe kutaka msaada wa mwenginewe.

46 Miongoni mwa Mayahudi kipo kikundi kazi yao kugeuza geuza maana ya maneno. Wao husema kimoyomoyo kumwambia Mtume s.a.w.: Tumesikia hayo maneno, na hatuifati hiyo amri. Na pia husema: Sikia maneno yetu - hukusikia wito. Wakikusudia kwa hayo kumuapiza Mtume. Na husema: Sikia bila ya kusikilizwa. Tamko hilo wanalipindua maana. Muradi wao ni kumuapiza, na wanajidai kuwa muradi wao ni kumwomba dua. Na husema: “Raai’na”, wakipindua ndimi zao wakijitia kuwa wanakusudia “Undhurna” yaani “Tuangalie”. Wanaonyesha kuwa wanataka uangalizi wake, na kumbe wanakusudia neno la Kiyahudi lenye maana ya “Mpumbavu” ili kuibeza Dini ya Kiislamu.

Na lau kuwa wangeliki nyooka sawa wakasema: “Tumesikia na tumet’ii” badala ya hiyo kauli yao ya “Tumesikia na tumeasi”, na wakasema: “Sikia” na wasiseme “Bila ya kusikilizwa”, na wakasema: “Undhurna” yaani “Tuangalie”, badala ya “Raa’ina”, ingeli kuwa bora kwao kuliko hayo wayasemayo, na ingeli kuwa ndiyo njia ya uadilifu zaidi. Lakini Mwenyezi Mungu amewatoa katika rehema yake kwa ule upinzani wao. Kwa hivyo huwaoni miongoni mwao wanao mwikitia mwenye kuwaitia Imani ila wachache tu.

47 Enyi mlio pewa Kitabu alichote remsha Mwenyezi Mungu! Iaminini Qur’ani tuliyo mteremshia Muhammad, inayo sadikisha mliyo nayo, kabla hatujawateremshia adhabu ya kufutwa nyuso zenu zikawa kama visogo, hazina pua, wala macho, wala nyusi. Au tukakutoeni katika rehema yetu kama tulivyo watoa wale walio ikhalifu amri yetu wakatenda waliyo katazwa ya kuvua samaki siku ya mapumziko, (Sabt au Sabato) siku ya Jumaamosi. Na hukumu ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutimizwa tu, wala hapana cha kuipinga.

48 Hakika Mwenyezi Mungu hafuti dhambi za ushirikina, kumfanya Yeye ana mshirika yeyote. Na husamehe dhambi zililo chini ya huo ushirikina kwa amtakaye miongoni mwa waja wake. Na mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu basi amemzulia Mwenyezi Mungu na ametenda dhambi kubwa mno isiyo stahiki kusamehewa.

49 Hustaajabii hali ya hao makafiri wanao zua kwa vitendo vyao? Vitendo vyao viovu wao wanaviona

- 50.** Tazama vipi wanavyo mzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na haya yatosha kuwa dhambi iliyo dhaahiri.⁵⁰
- 51.** Huwaoni wale walio pewa sehemu ya Kitabu? Wanaamini masanamu na Shet'ani! Na wanawasema walio kufuru, kuwa hao wameongoka zaidi katika njia kuliko Walio amini.⁵¹
- 52.** Hao ndio Mwenyezi Mungu amewalaani. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemlaani basi hutamwona kuwa na mwenye kumnusuru.⁵²
- 53.** Au wanayo sehemu ya utawala? Basi hapo wasingewapa watu hata tundu ya kokwa ya tende.⁵³
- 54.** Au wanawahusudu watu kwa yale aliyo wapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake? Basi tuliwapa ukoo wa Ibrahim Kitabu na hikima na tukawapa utawala mkubwa.⁵⁴
- 55.** Basi wapo miongoni mwao waliyo yaamini, na wapo walio yakataa. Na Jahannamu yatosha kuwa ni moto wa kuwateketeza.⁵⁵
- 56.** Hakika wale walio zikataa Ishara zetu tutawaingiza Motoni. Kila zitapo wiva ngozi zao tutawabadilishia ngozi nyengine ili waionje hiyo adhabu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.⁵⁶
- 57.** Na wale walio amini na wakatenda mema tutawaingiza katika Pepo zipitazo mito kati yake kwa kudumu humo milele. Huko watakuwa na wake walio takasika, na tutawaingiza katika vivuli vizuri kweli.⁵⁷

kuwa ni vizuri. Wanajisifu kuwa kwa vitendo hivyo wao wametakasika. Na ni Mwenyezi Mungu tu peke yake ndiye anaye jua jema na baya. Yeye ndiye wa kumtakasa amtakaye, na wala hamdhulumu mtu yeyote kadiri yake hata chembe.

50 Vipi watu hawa wanavyo mzulia Mwenyezi Mungu uwongo kwa haya na mengineyo mfano wa haya! Yatosha uwovu ulio wazi kwa huu uwongo wao kuyakashifu maovu yao.

51 Hebu huwastaajabii hawa walio pewa sehemu ya ujuzi wa Kitabu wanavyo ridhia ibada ya masanamu na Shetani, na wanavyo sema kuwa hao waabuduo masanamu ni afadhali wameongoka kwenye Njia kuliko Waislamu wenye kuamini?

52 Hao ndio alio watupa Mwenyezi Mungu na akawafukuzilia mbali kutoka kwenye rehema yake. Na mwenye kutupwa na Mwenyezi Mungu na akatolewa kwenye rehema yake basi kabisa huyo hana wa kumnusuru na kumlinda na ghadhabu ya Mola wake Mlezi.

53 Hao wamekoseshwa neema ya kuifuata haki, kama walivyo koseshwa na utawala. Na lau wakipewa utawala hawanufaishi watu hata chembe.

54 Na vipi watu hawa wanavyo waonea maya Waarabu? Na wakaona ni jambo kuu kuwa Mwenyezi Mungu alivyo wapa fadhila yake kwa kuwatolea Nabii kutokana nao, na ilhali Mwenyezi Mungu alimpa Ibrahim na ukoo wake - naye ni baba yenu (Mayahudi na Wakristo), na baba yao (Waislamu pia) - Kitabu kilicho teremshwa kwa ufunuo, na Unabii na Utawala ulio mkubwa!

55 Miongoni mwa walio pelekewa Nabii Ibrahim na ukoo wake wapo wenye kukiamini Kitabu kilicho teremshiwa kwao, na wapo walio kipa nyongo wakajitenga nacho. Na jaza ya hawa wenye kujitenga na wito wa Haki ni Jahannamu yenye moto wa kuteketeza.

56 Hakika wanao pinga hoja zetu zenye kubainisha wazi wazi, na wakawakanusha Manabii, tutakuja watia kwenye Moto utakao babua ngozi zao. Na kila zikisita kuhisi adhabu Mwenyezi Mungu atawabadilishia ngozi nyengine mpya ili machungu ya adhabu yabaki yakiendelea. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye ushindi katika mambo yake, na Mwenye hikima katika vitendo vyake. Humuadhibu mwenye kumpinga na akabaki na upinzani mpaka kufa kwake. (*Tazama Maelezo 4:56*)

57 Na ambao walio yasadiki yaliyo wajia kutoka kwa Mola wao Mlezi, na wakatenda vitendo vyema, tutawalipa kwa Imani yao na vitendo vyao na tutawaingiza katika Mabustani ya Peponi yapitayo mito chini ya miti yake. Uhai wao hauna kikomo kabisa. Nao humo watakuwa na wake walio t'ahirika na kila la aibu na uchafu. Tutawapa uhai wa starehe chini ya vivuli vizuri vya kudumu, waishi maisha mema yenye neema isiyo kwisha.

58. Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu. Hakika haya anayo kuwaidhini Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona.⁵⁸

59. Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema.⁵⁹

60. Huwaoni wale wanao dai kwamba wameamini yale yaliyo teremshwa kwako na yaliyo teremshwa kabla yako? Wanataka wakahukumiwe kwa njia ya upotofu, na hali wameamrisha wakatae hayo! Na Shet'ani anataka kuwapotezelea mbali.⁶⁰

61. Na wanapo ambiwa: Njooi kwenye yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, na njooi kwa Mtume; utawaona wanaafiki wanakukwepa kwa upinzani.⁶¹

62. Basi inakuwaje unapo wasibu msiba kwa sababu ya yale iliyo tanguliza mikono yao? Hapo tena hukujia wakiapa kwa Mwenyezi Mungu wakisema: Hatukutaka ila wema na mapatano.⁶²

63. Hao ndio wale ambao Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo ndani ya nyoyo zao. Basi waachilie mbali, uwape mawaidha na uwaambie maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao.⁶³

64. Na hatukumtuma Mtume yeyote ila at'iwe kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangeli kujia, wakamwomba Mwenyezi Mungu

58 Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni nyinyi Waumini mrejeshe vyote mlio pewa amana, kutokana na Mwenyezi Mungu au kutokana na watu, kwa wenyewe kwa uadilifu. Basi msifanye jeuri katika kuhukumu. Haya ni mawaidha yanayo toka kwa Mola wenu Mlezi. Basi yafanyieni pupa kuyafuata. Bora ya mawaidha ni yanayo tokana naye Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu daima ni Mwenye kusikia yasemwayo, ni Mwenye kuyaona yatendwayo. Basi anamjua anaye rejeshu amana, na anaye fanya khiana, na anaye hukumu kwa uadilifu, na anaye fanya jeuri. Na kila mmoja atamlipa kwa atendalo.

59 Enyi mlio sadiki aliyo kuja nayo Muhammad! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume, na wale wanao tawala mambo yenu miongoni mwa Waislamu wanao simama juu ya haki na uadilifu, na wanatekeleza Sharia ya Mwenyezi Mungu. Na mkizozana katika jambo baina yenu basi rejeeni kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake ili mpate kujua hukumu yake. Kwani Yeye Mwenyezi Mungu amekuteremshieni Kitabu chake na Mtume wake amebainisha hicho Kitabu. Na katika hayo ipo hukumu ya hayo mnayo khitalifiana kwayo. Haya ni kwa mujibu wa Imani yenu kumuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na haya ndio bora kwenu ili mpate kuongoka kwendea uadilifu katika mnayo khitalifiana kwayo, na mwisho wake ndio mzuri zaidi. Kwani hivyo ndio kuzuia zisitokee khilafu zinazo pelekea ugomvi na upotovu.

60 Ewe Nabii! Huwastaajabii hao wanao dai kuwa wanasadiki Kitabu ulicho teremshiwa wewe na vilivyo teremshwa kabla yako wewe, wanataka wahukumiwe katika ugomvi wao kwenye upotovu na uharibifu na hukumu isiyo kuwa ya Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu amekwisha waamrisha wayapinge hayo, wala wasitake kuhukumiwa kwa hayo. Na Shetani anataka awaachishe Njia ya Haki na Uwongofu, awapotezelee mbali.

61 Na wakiambiwa: Njooi kwenye Qur'ani na Sharia aliyo iteremsha Mwenyezi Mungu, na njooi kwa Mtume wake akubainishieni, utaona hao wanaafiki wanajitenga nawe kabisa wanakukataa.

62 Itakuwaje hali basi yakiwatereikia masaibu kwa sababu ya uovu wao na upotovu wa vitendo vyao, na wasipate pa kukimbilia ila kwako! Hapo basi watakuapia Mungu mbele yako kuwa wao hawakukusudia kwa maneno yao na vitendo vyao ila wema tu na kutaka mapatano.

63 Hao ndio wanao kula yamini kuwa hawakutaka ila wema na vitendo vya muwafaka. Mwenyezi Mungu anayajua vyema yaliyomo katika nyoyo zao, na anaujua uwongo wa hiyo kauli yao. Basi wewe usishughulike na maneno yao. Waite kwenye haki kwa mawaidha yaliyo mema, na sema nao maneno yenye hikima yenye kuathiri yanayo fika ndani ya nyoyo zao.

msamaha, na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangeli mkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu.⁶⁴

65. La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenykee kabisa.⁶⁵

66. Na lau kuwa tumewaamrisha: Jiueni, au tokeni majumbani kwenu, wasingeli fanya hayo ila wachache tu miongoni mwao. Na lau kama wangeli fanya walio waidhiwa ingeli kuwa bora kwao na uthibitisho wa nguvu zaidi.⁶⁶

67. Na hapo tunge wapa malipo makubwa kutoka kwetu.⁶⁷

68. Na tungeli waongoa Njia iliyo nyooka.⁶⁸

69. Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!⁶⁹

70. Hiyo ni fadhila itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kutosha.⁷⁰

71. Enyi mlio amini! Chukueni hadhari yenu! Na mtoke kwa vikosi au tokeni nyote pamoja!⁷¹

72. Na yupo kati yenu anaye bakia nyuma; na ukikusibuni msiba husema: Mwenyezi

64 Na Sisi hatukumtuma Mtume yeyote ila jambo lake kuu ni kuwa at'iwe, na ut'iifu huo ni kwa ruhusa iliyo toka kwa Mwenyezi Mungu. Na hakika mwenye kwenda kinyume, au kukanusha, au kukhaalifu, anakuwa ni mwenye kujidhulumu mwenyewe. Na lau kuwa hawa walio jidhulumu wakirejea kwenye uwongofu, wakakujia wakiomba msamaha kutokana na Mwenyezi Mungu kwa yale waliyo yatenda, na wewe ukawaombea msamaha kwa mujibu wa ujumbe wako na kwa ulivyo ona ilivyo geuka hali yao, basi hapana shaka watamkuta Mwenyezi Mungu, Aliye takasika na kutukuka, ni Mwingi wa kukubali toba, na Mwenye kuwarehemu waja wake.

65 Naapa kwa jina la Mola wako Mlezi! Hawahisabiwi kuwa ni Waumini wa Haki na wenye kuinyenyekea, mpaka watakapo kufanya wewe hakimu muamuzi wa mizozo inayo tokea baina yao. Kisha nafsi zao zisiane dhiki kwa utavyo hukumu, na wakunyenyeeke kama wanavyo nyenyekea Waumini wa kweli.

66 Na lau kuwa Sisi tumewalazimisha mashaka ya mwisho, kwa kuwaamrisha wapigane Jihadi moja kwa moja, na wajitolee nafsi zao kutilifu, au watoke nje waache majumba yao kwenda pigana Jihadi daima, wasinge kubali kut'ii ila wachache tu. Lakini Mwenyezi Mungu, Aliye takasika na kutukuka, hakalifishi ila linalo wezekana. Na lau kuwa wange fanya hayo na wakafuata haki yake ingeli kuwa ni kheri yao ya duniani na Akhera. Na hivyo ndiyo inavyo pelekea kuthibiti Imani, na kuingia imara, na kuleta utulivu.

67 Na lau kuwa wamesimama juu ya Haki alio ilazimisha Mwenyezi Mungu kwa kadri ya uweza wao, Mwenyezi Mungu angeli wapa malipo makubwa kwa fadhila yake.

68 Na kwa sababu ya kut'ii kwao kwa uweza wao inakuwa hakika Mwenyezi Mungu amewaongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka isio pindukia kiasi kwa kuzidi au kupungua.

69 Na mwenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume kwa kuzifuata kwa unyenyekevu amri zao na kuridhia hukumu yao, basi huyo yu pamoja na alio waneemesha Mwenyezi Mungu kwa uwongofu na kuwawezesha duniani na Akhera. Na watu hao ni Manabii wake, na wafuasi wao walio wasadiki na kuwakubali na wakafuata nyendo zao, na Mashahidi walio kufa katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na watu wema watendao mema kwa siri na dhaahiri. Na hapana la kushinda uzuri kuliko kuwa pamoja na watu hawa - haingii mashakani mwenye kukaa nao, wala hayachoshi mazungumzo yao.

70 Hayo ni makao matukufu kwa mwenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hiyo ni fadhila kubwa inayo tokana na Mwenyezi Mungu. Naye anavijua sana vitendo vyenu, naye atakulipeni kwavyo. Yamtosha Muumini kuwa Mwenyezi Mungu anamjua, naye lake ni kumt'ii Mola wake Mlezi na kutafuta radhi zake.

71 Enyi Mlio amini! Daima kuweni na hadhari na maadui wenu. Jizatitini kupambana na vitimbi vyao. Na mkitoka kwenda vitani tokeni kwa vikosi vikosi, au tokeni nyote pamoja.

Mungu kanifanyia kheri sikuwa nao.⁷²

73. Na ikikufikieni fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu husema - kama kwamba hapakuwa mapenzi baina yenu naye: Laiti ningeli kuwa pamoja nao nikafanikiwa mafanikio makubwa.⁷³

74. Basi nawapigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu wale ambao wanao uza uhai wa dunia kwa Akhera. Na anaye pigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu kisha akauliwa au akashinda basi tutakuja mpa ujira mkubwa.⁷⁴

75. Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanao onewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhaalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anaye toka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anaye toka kwako.⁷⁵

76. Walio amini wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na walio kufuru wanapiana katika njia ya upotofu. Basi piganeni na marafiki wa Shet'ani. Hakika hila za Shet'ani ni dhaifu.⁷⁶

77. Je, huwaoni wale walio ambiwa: Izuieni mikono yenu, na mshike Sala na mtoe Zaka. Na walipo amrishwa kupigana, mara kundi moja kati yao liliwaogopa watu kama kumwogopa Mwenyezi Mungu, au kwa khofu kubwa zaidi. Na wakasema: Mola Mlezi wetu! Kwa nini umetumrisha kupigana? Laiti unge tuakhirishia kiasi ya muda kidogo hivi! Sema: Starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa mwenye kuchamngu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi wa kokwa ya tende.⁷⁷

72 Na wahadharisheni wanao kaa nyuma wasende nanyi vitani. Miongoni mwa hao hao mnao ishi nao wakajizuia wasifuatane nanyi kwenda kupigana, mkipatwa na shida na masabu katika Jihadi, wao wa kikundi hicho, kwa kufurahia yaliyo kusibuni, husema: Mwenyezi Mungu katufanyia kheri kwa kuwa hatukwenda nao vitani.

73 Na mnapo pata fadhila ya ushindi kutokana na Mwenyezi Mungu, mkapata ngawira za vita, kikundi hicho hicho, kwa kuona maya na kutamani, husema: Laiti tungeli kuwa nao katika vita hivi, nasi tukapata mafanikio ya ngawira nzuri. Na husema haya na hayo kama kwamba hapakuwepo mapenzi yoyote yaliyo wafunga wao na nyinyi.

74 Ikiwa yupo kati yenu anaye bakia nyuma asende kupigana kutokana na udhaifu wa Imani yake, au ulegevu wa azma yake, basi na wapigane, kuinua Neno la Mwenyezi Mungu na kuwania Haki, wale walio uza uhai wao wa dunia kutafuta uhai wa Akhera. Na mwenye kupigana vita kwa ajili ya kunyanyua Neno la Mwenyezi Mungu na kuwania Haki, atapata moja ya mema mawili. Ama atauliwa apate fadhila ya kufa shahidi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, au atashinda, apate fadhila ya kufuzu katika dunia. Naye katika hali zote mbili atapewa na Mwenyezi Mungu ujira mkubwa katika Akhera.

75 Vipi inakufalieni kuwa msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na hali wanyonge, wanaume na wanawake na watoto wao, wanayayatika kuomba msaada wa kuwanusuru, huku wakimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu wakisema: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutoe kwenye utawala wa hawa madhaalimu, na kwa nguvu zako na rehema yako tuwezeshe tuwe chini ya utawala wa Waumini; na tujaalie kutoka kwako mgombozi wa kutunusuru!

76 Walio isadiki Haki na wakaifuata, hupigana kwa ajili ya kulitukuza Neno la Mwenyezi Mungu, na uadilifu, na Haki. Na wale wanao pinga wakafanya inadi hupigana kwa ajili ya dhulma na uharibifu. Kwa hivyo hawa wamekuwa ni vipenzi vya Shetani. Basi enyi Waumini! Wapigeni vita hao, kwani wao ni wenzake Shetani na wasaidizi wake. Na jueni kuwa nyinyi mtawashinda tu kwa kuungwa mkono na Mwenyezi Mungu, kwani mpango wa Shetani, na ingawa mkubwa vipi ufisadi wake, ni dhaifu, hauna nguvu. Na Haki ndiyo yenye ushindi.

77 Ewe Muhammad! Hebu huwaangalii ukawastaajabia wale walio taka kupigana kabla ya kuja ruhusa, wakaambiwa: Bado haujafika wakati wa vita. Basi izuieni mikono yenu msipigane. Bali shughulikieni kushika Sala, na kutoa Zaka. Na Mwenyezi Mungu alipo waamrisha wapigane kikawa kikundi kimoja kati yao kikawa kinawaogopa watu kama kumkhofu Mwenyezi Mungu, au zaidi. Wakasema kwa kuona ni mageni hayo: Kwa nini ukatumrisha kupigana? Wao walidhani kuwa kuamrisha vita kunahimiza ajali

78. Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu. Na likiwafikilia jema wanasema: Hili limetoka kwa Mwenyezi Mungu. Na likiwafikilia ovu wanasema: Hili limetoka kwako wewe. Sema: Yote yanatokana na Mwenyezi Mungu. Basi wana nini watu hawa hata hawakaribii kufahamu maneno?⁷⁸

79. Jema lilio kufikia limetokana na Mwenyezi Mungu. Na ovu lilio kusibu linatokana na nafsi yako. Nasi tumekutuma kwa watu uwe ni Mtume. Na Mwenyezi Mungu ni shahidi wa kutosha.⁷⁹

80. Mwenye kumt'ii Mtume basi ndio amemt'ii Mwenyezi Mungu. Na anaye kengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao.⁸⁰

81. Na wanasema: Tunat'ii. Lakini wanapo toka kwako kundi moja miongoni mwao hupanga njama usiku kinyume na unayo yasema. Na Mwenyezi Mungu anayaandika yote hayo wanayo yapangia njama za usiku. Basi waachilie mbali, na umtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mtegemewa wa kutosha.⁸¹

82. Hebu hawaizingatii hii Qur'ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.⁸²

yao, na kwa hivyo wakasema: Hebu lau ungelitungojea muda kidogo tupate kustarehe na ulimwengu! Waambie: Songeni mbele mkapigane hata ikiwa mtakufa mashahidi, kwani starehe ya dunia, ingawa ni kubwa vipi, ni chache ukilinganisha na starehe ya Akhera. Na Akhera ni bora na kubwa zaidi kwa mwenye kumcha Mwenyezi Mungu, na huko mtakuja lipwa kwa vitendo vyenu vya duniani, wala hampunguziwi hata chembe katika ujira wenu.

78 Hakika hayo mauti mnayo yakimbia yatakututeni popote pale mlipo, na hata mkikaa ndani ya ngome zilizo jengwa madhubuti imara. Na hao wenye imani legevu na dhaifu husema pindi wapatao ushindi na ngawira: Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu. Na pindi wapatao lawama au kushindwa wao hukwambia wewe: Ewe Muhammad! Haya yanatokana na wewe. Haya si lolote ila kukufanya kuwa wewe ni mkorofi, na kukutopia lawama wewe badala ya nafsi zao. Basi waambie: Kila linalo kupatani, mnalo lipenda na mnalo lichukua, linatokana na kudra ya Mwenyezi Mungu, na linatokana na majaribio yake na mitihani yake. Wana nini watu hawa madhaifu hata hawajakaribia kujua usawa wa maneno wanayo ambiwa?

79 Ewe Nabii! Kufanikiwa, na neema, na afya, na salama unayo ipata inatokana na fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako. Yeye anafanya haya kukufadhili kukufanyia hisani. Na inapo kusibu shida, na mashaka, na udhiya, na ya karaha, basi yanatokana na nafsi yako mwenyewe kwa sababu ya upungufu fulani au makosa uliyo yatenda. Haya anaambiwa Mtume s.a.w. ni kama mfano wa wanaadamu wote ijapo kuwa halikutokea kwake la uovu. Kwani Mtume anaambiwa: Tumekutuma kuwa Mtume kutoka kwetu kwa watu wote. Na Mwenyezi Mungu ni shahidi wa kufikisha kwako huo ujumbe na juu ya kuitikia kwao hao watu. Na Yeye ni Mjuzi wa kutosha.

80 Mwenye kumt'ii Mtume basi ndio amemt'ii Mwenyezi Mungu, kwani yeye haamrishi ila alichu amrisha Mwenyezi Mungu. Wala hakatazi ila alichu kataza Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo kumt'ii yeye (Mtume s.a.w.) ndio kutenda na kuacha kwa ut'iifu wa Mwenyezi Mungu. Na mwenye kukataa kukut'ii wewe basi, kwani Sisi hatukukupeleka wewe ila uwe ni mbashiri na mwonyaji tu, sio uwe ni mlinzi wao na muangalizi wao, uwalindie vitendo vyao. Hayo ni yetu Sisi sio yako.

81 Na kikundi hichi kinacho tapatapa husema: Amri yako tunait'ii. Hatuna kwako ila kut'ii unayo amrisha na kukataza. Lakini wakisha toka kwako wakawa mbali nawe, baadhi yao hupanga vijambo vyao usiku usiku, kinyume na unavyo waambia ya kuwaamrisha na kuwakataza. Na Mwenyezi Mungu, *Subhanahu wa Taa'la*, Aliye takasika na Kutukuka, anayadhibiti yote wanayo yapanga kwa siri. Basi usiwashughulikia, na wapuuze, na mwachie mambo yao Mwenyezi Mungu, na wewe mtegemee Yeye. Na Mwenyezi Mungu ni wa kutosha kuwa ni Mtegemewa wako, na Mlinzi wako wa kumwachilia mambo yako yote.

82 Basi hao wanaafiki hawazingatii Kitabu cha Mwenyezi Mungu wakajua hoja za Mwenyezi Mungu zilizo juu yao kuwa ni waajibu kut'ii na kufuata amri yako? Na kwamba Kitabu hichi kinatoka kwa Mwenyezi Mungu kwa yalivyo shikamana maana yake na hukumu zake, na kinavyo fungamana wenyewe kwa wenyewe? Hii ni dalili kuwa ni kweli kinatoka kwa Mwenyezi Mungu, kwani lau kuwa

83. Na linapo wafikia jambo lolote lilio khusu amani au la kitisho wao hulitangaza. Na lau kuwa wangeli lipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wale wanao chunguza wangeli lijua. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake mngeli mfuata Shet'ani ila wachache wenu tu.⁸³

84. Basi pigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Hukalifishwi ila nafsi yako tu. Na wahimize Waumini. Huenda Mwenyezi Mungu akayazuia mashambulio ya walio kufuru. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mkali zaidi wa kushambulia na Mkali zaidi wa kuadhibu.⁸⁴

85. Mwenye kusaidia msaada mwema ana fungu lake katika hayo, na mwenye kusaidia msaada mwovu naye ana sehemu yake katika hayo. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza na ujuzi juu ya kila kitu.⁸⁵

86. Na mnapo amkiwa kwa maamkio yoyote, basi nanyi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuhisabu kila kitu.⁸⁶

87. Mwenyezi Mungu, hapana mungu isipo kuwa Yeye. Kwa yakini atakukusanyeni Siku ya Kiyama. Halina shaka hilo. Na ni nani msema kweli kuliko Mwenyezi Mungu?⁸⁷

88. Mmekuwaje kuwa makundi mawili kwa khabari ya wanaafiki, na hali Mwenyezi Mungu amewageuza kwa sababu ya yale waliyo yachuma? Je! Mnataka kumwona mwongofu ambaye Mwenyezi Mungu amemhukumu kuwa kapotea? Na aliye mhukumu Mwenyezi Mungu kuwa amekwisha potea wewe hutampatia njia.⁸⁸

kinatokana na mwengine weni basi maana yake yangeli gongana, na hukumu zake zingeli khitalifiana sana. 83 Na hichi kikundi cha wanaafiki kikipata khabari zozote zililo khusu nguvu au udhaifu wa Waislamu huzitangaza na kuzieneza nje, ili kuwababaisha Waislamu au kuwatia khofu katika nyoyo zao, au ili zifike khabari zao kwa maadui wao. Na lau kuwa hawa wanaafiki watangazao wamerudisha jambo lililo khusu usalama au kitisho kwa Mtume na kwa wakuu wa mambo miongoni mwa waongozi na Masahaba wakubwa, wakataka kwao kujua hakika, wangeli jua hao wanao jitahidi kuchungua mambo na kuyatangaza, kuwa yaliyo kweli yanatokana na Mtume na waongozi wengine. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu kwa alivyo zithibitisha nyoyo zenu juu ya Imani, na kuzuia fitina, na rehema yake kwa kukupeni sababu na njia za ushindi, wengi wenu wangeli fuata upotovu wa Shetani, na wasingeli okoka kutokana na upotovu wake ila wachache tu.

84 Na kama wapo kati yenu mfano wa hawa wanaafiki basi wapuuzilie mbali. Na wewe pigana kwa ajili ya Neno la Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya Haki. Wewe huna jukumu ila la nafsi yako tu. Kisha waite Waumini wende vitani, na wahimize. Huenda Mwenyezi Mungu kwa kupitia kwako na kwao akazuia hayo mashambulio ya makafiri. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukuungeni mkono, na ni Mwenye kukunusuruni. Na Yeye ana nguvu kuliko wote, na mkali kuliko wote katika kuwaadhibu makafiri.

85 Na hawa wanaafiki husaidia ufisadi, na watu wa Imani husaidia Haki. Na mwenye kusaidia jambo jema ana fungu lake la thawabu. Na mwenye kuwasaidia watu waovu naye ana mzungo wake wa dhambi katika malipo yake. Na Mwenyezi Mungu ana uweza juu ya kila kitu, na Mwenye kujua kila kitu.

86 Akikuamkieni mtu yeyote kwa maamkio ya salamu, au dua, au ya namna yoyote ya hishima, au namna nyengine yoyote ile, basi mjibuni kwa maamkio yaliyo mazuri zaidi, au kwa uchache mjibuni kama alivyo kuamkieni yeye. Kwani hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kutia hisabuni kila kitu, kikubwa na kidogo.

87 Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu ila Yeye, wala hapana mwenye uweza ila Yeye, hapana shaka atakufufueni baada ya kufa kwenu, na atakukusanyeni kwenye kituo cha kuhisabiwa kwa ajili ya malipo. Hayo hayana shaka. Yeye anasema hayo, basi msiyatilie shaka maneno yake. Na kauli gani iliyo ya kweli zaidi kuliko kauli ya Mwenyezi Mungu.

88 Haikufaliini, enyi Waumini, kukhitalifiana katika mas-ala yaliyo khusu wanaafiki, ambao wanadhihirisha Uislamu na wanaficha ukafiri. Haikufaliini kukhitalifiana kwa mas-ala yao, kuwa ati wao ni Waumini au makafiri? Wauwawe au waachiliwe? Je, wameelekea kuongoka au hawatarajiwi uwongofu? Fahamu zao

89. Wanapenda lau kuwa nanyi mnge kufuru kama walivyo kufuru wao, ili muwe sawa sawa. Basi msiwafanye marafiki miongoni mwao mpaka wahame kwa ajili ya Dini ya Mwenyezi Mungu. Na wakikengeuka basi wakamateni na wauweni popote mnapo wapata. Wala msimfanye rafiki katika wao wala msaidizi.⁸⁹

90. Isipokuwa wale walio fungamana na watu ambao mna ahadi baina yenu na wao, au wanakujieni na vifua vyao vina dhiki kupigana nanyi, au kupigana na watu wao. Na lau angeli penda Mwenyezi Mungu angeli wasaliti juu yenu wakapigana nanyi. Basi wakijitenga nanyi, wasipigane nanyi, na wakakuleteeni amani, basi Mwenyezi Mungu hakukupeni njia kupigana nao.⁹⁰

91. Mtawakuta wengine wanataka wapate salama kwenu na salama kwa watu wao. Kila wakirudishwa kwenye fitna hudidimizwa humo. Ikiwa hawajitengi nanyi, na wakakuleteeni salama, na wakazuia mikono yao, basi wakamateni na wauweni popote mnapo wakuta. Na juu ya hao ndio tumekupeni hoja zilizo wazi.⁹¹

92. Na haiwi Muumini kumuwa Muumini ila kwa kukosea. Na mwenye kumuwa Muumini kwa kukosea basi amkomboe mtumwa aliye Muumini, na atoe diya kuwapa jamaa za maiti, isipo kuwa waache wenyewe kuwa ni sadaka. Na akiwa ni jamaa wa maadui zenu, hali yeye ni Muumini, basi ni kumkomboa mtumwa aliye Muumini. Na akiwa ni miongoni wa watu ambao pana ahadi baina yenu na wao basi wapewe diya watu wake na akombolewe mtumwa Muumini. Na asiye pata, basi afunge miezi miwili mfululizo, kuwa ni toba kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima.⁹²

zimegeuzwa kwa yaliyo chumwa na vitendo vyao. Shari imekuwa ndio inayo wahukumu, basi usimtarajie kuongoka yule ambaye Mwenyezi Mungu kwa ujuzi wake wa tangu na tangu kesho mkadiria asiongoke. Kwani aliye andikwa katika ujuzi wa Mwenyezi Mungu wa tangu azali kuwa ni mwenye kupotea basi huna njia ya kumwongoa.

89 Hakika nyinyi mnapenda kuwaongoa hawa wanaafiki, na wao wanapenda nyinyi mkufuru kama wao, ili muwe nyote sawa kwa ukafiri. Ilivyo kuwa hivyo basi msitake wa kukuungeni mkono miongoni mwao. Wala msiwafanye wenzenu, mpaka wakubali kutoka huko kwao kuwania Jihadi kwa ajili ya Uislamu. Hivyo tu ndio itawatoka sifa ya unaafiki. Lakini wakiyakataa hayo, wakaungana na maadui zenu, basi wauweni popote mtapo wapata, wala msiwaone kuwa ni wenzenu, wala msiwachukulie kuwa ndio wasaidizi wenu.

90 Katika wanaafiki, wanao stahiki kuuliwa kwa fisadi yao kuwafisidi umma wa Waumini, watoe wale ambao wamefungamana na kaumu ambao baina yao na Waumini yapo mapatano ya kuzuia kuuliwa aliye fungamana na upande mmoja wapo. Au vile vile ambao wametatizwa hawajui wapigane pamoja na watu wao, ambao ni maadui wa Waislamu wasio na mkataba nao, au wapigane pamoja na Waumini? Kwani hakika wale wa kwanza inakatazwa kuwauwa kwa ajili ya mkataba, na wengine inakatazwa kuwauwa kwa kuwa hawajui moja wapo la kutenda. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amependa angeli wajaalia hao wakupigeni vita. Ilivyo kuwa wamekhiari kukaa tu wasikupigeni na wakaingiana nanyi kwa salama na amani, basi haikufaliini nyinyi kuwauwa. Hapana ruhusa kufanya hayo.

91 Mkiwashinda washirikina, hao wanaafiki huwa pamoja nanyi; na washirikina wakiwashinda Waislamu, wao huwa pamoja na washirikina. Wao hutaka wapate amani kwa Waislamu na wapate amani kwa jamaa zao washirikina. Hawa wamo katika upotovu na unaafiki wa moja kwa moja. Ikiwa hawatoacha kukupigeni vita na wakakutangazieni amani na salama, basi wauweni popote muwapatapo. Kwani kwa kuto kujitenga na kukupigeni vita, basi inakuwa Waumini wana haki kuwauwa. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amewapa Waumini hoja iliyo wazi kuwapiga vita.

92 Kuwagawa wanaafiki namna hii ni kwa ajili ya kutoka shakani, ili Muumini asimuuwe Muumini mwenziwe kwa kumdhania kuwa ni mnaafiki. Na haijuzu kumuwa Muumini ila kwa kukosea, bila ya kukusudia. Na katika hali ya kumuwa Muumini kwa kukosea akiwa anaishi chini ya utawala wa dola ya Kiislamu, basi atatoa muuwaji diya kuwapa walio fiwa kuwa ni fidia kwa mtu waliye mkosa, na

93. Na mwenye kumuuwa Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu humo atadumu, na Mwenyezi Mungu amemkasirikia, na amemlaani, na amemuandalia adhabu kubwa.⁹³

94. Enyi mlio amini! Mnapo safiri katika Njia ya Mwenyezi Mungu basi hakikisheni, wala msimwambie anaye kutoleeni salamu: Wewe si Muumini; kwa kutaka manufaa ya maisha ya dunia hii, hali ya kuwa kwa Mwenyezi Mungu zipo ghanima nyingi. Hivyo ndivyo mlivyo kuwa nyinyi zamani, na Mwenyezi Mungu akakuneemesheni. Basi chunguzeni sawa sawa. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.⁹⁴

95. Hawawi sawa Waumini wanao kaa tu wala hawanadharura, na wale wanao pigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Mwenyezi Mungu amewatukuza cheo wale wanao pigana kwa mali yao na nafsi zao kuliko wale wanao kaa tu. Ingawa Mwenyezi Mungu amewaahidi wote mashukio mema, lakini Mwenyezi Mungu amewafadhili wanao pigana kwa ujira mkubwa kuliko wanao kaa tu.⁹⁵

96. Ni vyeo hivyo vinavyo toka kwake, na maghfira na rehema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira na Mwenye kurehemu.⁹⁶

97. Hakika Malaika watawaambia wale ambao wamewafisha nao wamejidhulumu nafsi zao: Mlikuwa vipi? Watasema: Tulikuwa tunaonewa. Watawaambia: Kwani ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa na wasaa wa kuhamia humo? Basi hao makaazi

tena amkomboe mtumwa aliye Muumini iwe ni kuwafidia umma wa Kiislamu kwa walicho kosa. Kwani kumkomboa Muumini ni kama kumhuisha mtu kwa kumpatia uhuru. Inakuwa kwa kukomboa shingo ya Muumini ni kuulipa umma wa Kiislamu kwa walicho kosa.

Ikiwa aliye uliwa yumo katika watu ambao wana mapatano ya amani na Waislamu, basi yapasa kumpa uhuru mtumwa na kuwalipa watu wa maiti diya, kwani inakuwa hawaichukui hiyo diya kwa kuwaudhi Waislamu kwa sababu ya mapatano yao. Na ikiwa mwenye kuuwa bila ya kukusudia hakupata mtumwa Muumini wa kumkomboa, basi afunge miezi miwili mfululizo, asile mchana hata siku moja. Hayo yawe ni kuitengeza nafsi na kujizoosha kuwa na hadhari zaidi. Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika na Aliye tukuka anazijua sana nafsi za watu na niya zao. Naye ni Mwenye hikima, anajua kuzipanga adhabu zake. (*Tazama Maelezo 4:92*)

93 Hakika mwenye kumuuwa Muumini kwa mauwaji ya kukusudia na kuona ndio ndivyo mauwaji hayo, jaza yake inayo lingana na ukhalifu huo ni kuingizwa Motoni milele, na kughadhibikiwa na Mwenyezi Mungu na afukuzwe kutokana na rehema yake. Na Mwenyezi Mungu amemtengezea Akhera adhabu kubwa, kwani kitendo hichi ndio ukhalifu mkubwa kabisa katika dunia.

94 Kutahadhari msije mkamuuwa Muumini ni waajibu katika wakati wa kwenda vitani. Mkisafiri kwa ajili ya Jihadi ya Njia ya Mwenyezi Mungu jijuvyeni hakika ya hao mnao pigana nao kabla ya kupambana. Je, hao wamesilimu au bado ni washirikina. Wala msimwambie anaye kutoleeni salamu kuwa ni ishara ya amani: Wewe si Muumini, kwa kuwa mnataka kumnyang'anya mali yake na kondoo wake. Bali ipokeeni salamu yake, kwani kwa Mwenyezi Mungu amekuahidini kupata ngawira nyingi nyenginezo. Na nyinyi, enyi Waumini! Mlikuwa hivyo hivyo katika ukafiri kabla ya hayo, na Mwenyezi Mungu amekuhidini. Basi hakikisheni mambo ya hao mnao wakuta. Na Mwenyezi Mungu anajua baraabara, na hapana chochote kinacho fichikana kwake. Na Yeye hakika ni Mwenye kuhisabu kwa mujibu wa ujuzi wake.

95 Na hakika Jihadi pamoja na kuchukua hadhari inayo takikana ina fadhila kubwa sana. Basi hawawi sawa wanao kaa majumbani mwao wasende kupigana Jihadi na wale Mujaahidiina, wanao pigana kwa mali yao na nafsi zao. Kwani Mwenyezi Mungu amewanyanya wale Mujaahidiina daraja, cheo cha juu kuwashinda wale wanao kaa nyuma; ila ikiwa wale wanao kaa nyuma wana udhuru unao wazuia kutoka kwenda vitani. Hapo inakuwa udhuru wao unawatoa lawamani, juu ya kuwa wanao pigana wana fadhila na cheo makhsusi. Mwenyezi Mungu amewaahidi makundi yote mawili mashukio mema, na matokeo mazuri.

96 Na cheo hichi walicho khusishwa nacho hao wanao pigana Jihadi ni cheo kikubwa, cha juu, hata imekuwa ni kama cheo cha kutafautisha sana baina yao na wengineo. Na kwa ajili ya cheo hichi watapata maghfira makubwa na rehema kunjufu.

yao ni Jahannamu, nayo ni marejeo mabaya kabisa.⁹⁷

98. Isipo kuwa wale walio kuwa wanyonge miongoni mwa wanaume na wanawake na watoto wasio na uweza wa hila ya kuongoza njia ya kuhama.⁹⁸

99. Basi hao huenda Mwenyezi Mungu akawasamehe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa maghfira.⁹⁹

100. Na mwenye kuhama katika Njia ya Mwenyezi Mungu atapata pengi duniani pa kukimbilia, na atapata wasaa. Na anaye toka nyumbani kwake kuhama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kisha yakamfika mauti njiani basi umethibiti ujira wake kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu.¹⁰⁰

101. Na mnapo safiri katika nchi si vibaya kwenu kama mkifupisha Sala, iwapo mnachelea wasije wale walio kufuru wakakuleteeni maudhi. Hakika makafiri ni maadui zenu walio wazi wazi.¹⁰¹

102. Na unapo kuwa pamoja nao, ukawasalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe na wachukue silaha zao. Na watakapo maliza sijida zao, basi nawende nyuma yenu, na lije kundi jingine ambalo halijasali, lisali pamoja nawe. Nao wachukue hadhari yao na silaha zao. Walio kufuru wanapenda mghafilike na silaha zenu na vifaa vyenu ili wakuvamieni mvamio wa mara moja. Wala si vibaya kwenu ikiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mkawa wagonjwa, mkaziweka silaha zenu. Na chukueni hadhari yenu. Hakika Mwenyezi Mungu amewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha.¹⁰²

97 Na hakika ni waajibu wa Muislamu kuhamia kwenye dola ya Kiislamu asiishi katika udhalili. Malaika watawauliza wakisha kufa: Mlikuwa je hata mkaridhia maisha ya unyonge na kudharauliwa? Na wao watajibu: Tulikuwa wanyonge katika nchi hiyo tukionewa. Malaika watawambia: Kwani ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa kunjufu ina wasaa, mkaweza kuhama badala ya kuishi katika uonevu? Watu hao wanao kubali uonevu, na wao wanaweza kuondoka, makao yao yatakuwa ni Jahannamu. Na hayo ni mashukio maovu kabisa. Basi Muislamu haimfalii kuishi katika udhalili, bali aishi na utukufu wake na hishima yake.

98 Juu ya hivyo wanasameheka na adhabu hii wale wasio weza kusafiri miongoni mwa wanaume, na wanawake, na watoto, wasio na nguvu, na hawana hila, wala hawakupata njia ya kutoka.

99 Na hao wanatarajiwa kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu. Na ni shani yake Mwenyezi Mungu kusamehe na kughufiria.

100 Anaye hama kutafuta njia za kuiwania Haki na kuiunga mkono, atakuta duniani kwingi endako ambako maadui wa Haki wanahizika. Na atapata wasaa wa uhuru, na makao ya hishima, na thawabu, na ujira mkubwa. Aliye toka kwake kuhamia dola ya hishima, ambayo ndiyo dola ya Mwenyezi Mungu na Mtumewe, kisha yakamdiriki mauti kabla hafafika endako, basi ujira wake umethibiti. Mwenyezi Mungu amemkirimu kwa kujiwajibishia kumlipa ujira wake, na kumghufiria na kumrehemu. Ni shani yake kughufiria na kurehemu.

101 Sala ni faridha isiyo epukika. Haiachiki Sala kwa ajili ya safari, lakini hana dhambi anaye fupisha Sala safarini. Watokao kwenda safari wakikhofia kuwa makafiri watawaletea ya kuwaudhi, wanaweza kufupisha Sala. Sala za rakaa nne zisaliwe rakaa mbili. Kutahadhari na kuingiliwa na makafiri ni waajibu, kwani wao ni maadui, na uadui wao uwazi.

102 Ewe Nabii Muaminifu, ukiwa nao na Sala ya Jamaa inasaliwa, msisahau kutahadhari na maadui. Na hayo ni kuwagawa Waislamu makundi mawili. Moja lianze kusali kwa kukufuata wewe, na wakati huo la pili lisimame kwa hadhari na silaha likilinda vifaa. Ukisha nusu ya Sala, kundi lililo sali nawe lende nyuma yako, na lije jengine lisali nawe Sala iliyo bakia. Kisha litimize sehemu waliyo ikosa. Na lile la kwanza lisali baki ya Sala. Na hii huitwa “Laahiqah”, yaani iliyo kutwa (1) na nyengine inaitwa “Masbuuqah”, yaani iliyo tanguliwa, kwa kuwa inasaliwa mwanzo wa Sala ya Jamaa; na “Laahiqah” inasaliwa mwisho wa Sala ya Jamaa. Mpango huu ni kwa sababu isikosekane Sala, na kutahadhari na

- 103.** Mkisha sali basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu mkisimama, na mkikaa, na mnapo jinyoosha kwa kulala. Na mtapo tulia basi shikeni Sala kama dasturi. Kwani hakika Sala kwa Waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalumu.¹⁰³
- 104.** Wala msifanye ulegevu kuwafukuzia kaumu ya maadui. Ikiwa mnaumia, basi nao pia wanaumia kama mnavyo umia nyinyi. Nanyi mnataraji kwa Mwenyezi Mungu wasio yataraji wao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima.¹⁰⁴
- 105.** Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa haki ili upate kuhukumu baina ya watu kwa alivyo kuonyesha Mwenyezi Mungu. Wala usiwe mtetezi wa makhaaini.¹⁰⁵
- 106.** Na muombe maghfira Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, Mwenye kurehemu.¹⁰⁶
- 107.** Wala usiwatete wanao khini nafsi zao. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi aliye khaaini, mwenye dhambi.¹⁰⁷
- 108.** Wanataka kujificha kwa watu, wala hawataki kujificha kwa Mwenyezi Mungu, naye yu pamoja nao pale wanapo panga njama usiku kwa maneno asiyo yapenda. Na Mwenyezi Mungu anayajua vyema wanayo yatenda.¹⁰⁸
- 109.** Hivyo nyinyi mmewatetea hawa katika uhai huu wa duniani. Basi nani atakaye watetea kwa Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama? Au ni nani atakuwa wakili wao wa kumtegemea?¹⁰⁹
- 110.** Na anaye tenda uovu au akajidhulumu nafsi yake, kisha akaomba maghfira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, Mwenye

makafiri ambao wanapenda mghafilike na silaha zenu na vifaa vyenu wapate kukuvamieni kwa ghafla, na wakumalizeni nanyi mmo katika Sala. Vita na washirikina ni waajibu, na havina ukomo. Lakini hapana dhambi juu yenu kusita kwa ajili ya udhuru kama mvua au maradhi, juu ya kuwa lazima muwe na hadhari ya kudumu. Na hii ni adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa makafiri hapa duniani, na Akhera amewaandalia adhabu ya fedheha na udhalili. (Tazama Maelezo 4:102)

103 Na mkisha Sala ya vita, inayo itwa Sala ya Khofu, msisahau kumkumbuka Mwenyezi Mungu daima. Mkumbukeni nanyi mmesimama, mnapihana, mmekaa, na mmelala. Kwani kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu kunatia nguvu nyoyo, na kuzituliza. Khofu ikiondoka pakawa na utulivu basi timizeni Sala kwa ukamilifu, kwani Sala imefaridhiwa juu ya Waumini isaliwe kwa nyakati zake.

104 Msilegee kuwafukuzia makafiri walio kwisha kukutangazieni vita na wanajaribu kukushambulieni kila pahala. Hakika vita havikosi maumivu. Ikiwa nyinyi Waumini mmepea majaraha na mengineyo, na wao makafiri pia wameyapata machungu. Khitilafu yenu ni kuwa wao hawapiganii Haki, wala hawataraji kitu kwa Mwenyezi Mungu; na nyinyi mnataka Haki na mnataraji radhi za Mwenyezi Mungu na neema za kudumu. Na Mwenyezi Mungu anavijua vitendo vyenu na vyao, naye ni Mwenye hikima, anamlipa kila mtu kwa alitendalo.

105 Tumekuteremshia hii Qur'ani kwa haki na kwa kweli. Imekusanya kila lililo la haki. Inabainisha haki mpaka Siku ya Kiyama, ili iwe ni taa yako ya kukupa mwangaza kuwahukumu watu. Basi hukumu baina yao, wala usiwepigania walio makhaaini.

106 Na unapo hukumu baina ya watu muelekee Mwenyezi Mungu, na ukumbuke utukufu wake, na uombe maghfira yake na rehema yake. Kwani kughufiria na kurehemu ndio shani yake *Subhanahu wa Taa'la*.

107 Wala usiwatete wale wanao fanya khiana, na wakaendelea mno katika kuificha hiyo khiana katika nafsi zao. Kwani Mwenyezi Mungu hampendi ambaye mtindo wake ni khiana na kufanya madhambi.

108 Wanajificha, na wanataka kujisitiri kwa watu wasiione khiana yao. Wala hayumkini kuzificha khiana zao kwa Mwenyezi Mungu, na ilhali Yeye daima yu pamoja nao. Na wao usiku usiku hukubaliana kwa maneno yasiyo mridhi Mwenyezi Mungu ya kuwasingizia tuhuma watu wasio na makosa. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu anajua vyema, na hapana kitu kinacho weza kujificha na ujuzi wake.

109 Ikiwa nyinyi mnawatetea hao wakosa wasipate adhabu ya duniani, basi hatopatikana wa kuwatetea Siku ya Kiyama mbele ya Mwenyezi Mungu na kukubali kuwa ni mlinzi wao wa kuwasaidia.

kurehemu.¹¹⁰

111. Na anaye chuma dhambi, basi ameichumia nafsi yake mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hikima.¹¹¹

112. Na atendaye kosa au dhambi kisha akamsingizia asiye na kosa, basi amejitwika dhulma na dhambi iliyo wazi.¹¹²

113. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako na rehema yake, kundi moja kati yao linge dhamiria kukupoteza. Wala hawapotezi ila nafsi zao, wala hawawezi kukudhuru kwa lolote. Na Mwenyezi Mungu amekuteremshia Kitabu na hikima na amekufundisha uliyo kuwa huyajui. Na fadhila za Mwenyezi Mungu zilizo juu yako ni kubwa.¹¹³

114. Hakuna kheri katika mengi ya wanayo shauriana kwa siri, isipo kuwa kwa yule anaye amrisha kutoa sadaka, au kupatanisha baina ya watu. Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi tutakuja mpa ujira mkubwa.¹¹⁴

115. Na anaye mpinga Mtume baada ya kumdhahirikia uwongofu, na akafuata njia isiyo kuwa ya Waumini, tutamuelekeza aliko elekea, na tutamuingiza katika Jahannamu. Na hayo ni marejeo maovu.¹¹⁵

116. Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi kushirikishwa na kitu. Lakini Yeye husamehe yasiyo kuwa hayo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi huyo amepotea upotovu wa mbali.¹¹⁶

110 Mlango wa toba, hakika, uwazi. Anaye tenda kitendo kiovu cho chote, au akajidhulumu nafsi yake kwa kufanya maasi, kisha akamtaka msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu, atamkuta Mwenyezi Mungu yu tayari kukubali toba yake, na kumghufiria madhambi yake. Kwani ndio mwendo wake Mwenyezi Mungu kughufiria na kurehemu.

111 Hakika madhara ya madhambi ni juu ya yule yule ayatendayo. Mwenye kuchuma madhambi basi anajidhuru mwenyewe. Na alitendalo linamuangukia mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika na kutukuka anajua aliyo yatenda, na amachukulia kwa mujibu wa hikima yake. Atamuadhibu au atamsamehe kwa mujibu wa hikima yake.

112 Na mwenye kutenda makosa na madhambi kisha akamsingizia mwengine asiye na kosa alilo litenda - kama vile mwizi kaiba kitu kisha akamsingizia wizi mtu mwengine - mtu huyo ana dhambi mbili. Moja ni uwongo na uzushi, na la pili lile kosa lilio wazi la kwiba.

113 Lau kuwa Mwenyezi Mungu hakukufadhili kwa kuteremshia Wahyi, Ufunuo, na akakupa rehema ya kutambua na kufahamu hakika, kikundi cha wapotovu kingependa kukupoteza. Lakini hawapotezi ila nafsi zao. Kwani Mwenyezi Mungu ni muangalizi wako, na ndiye mwenye kukuonyesha haki. Hayakufikilii madhara ya mipango yao na upotezi wao. Yeye Mwenyezi Mungu amekuteremshia Qur'ani Tukufu ambayo hiyo ndiyo mizani ya haki, na ameutuza moyo wako kwa hikima, na amekufundisha Sharia na hukumu ambazo ulikuwa hukuzijua ila kwa kufunuliwa na Yeye. Hakika fadhila za Mwenyezi Mungu juu yako daima ni kubwa.

114 Hakika wale wanao kaa wakipanga mambo yao kisirisiri, mambo hayo hayana kheri, kwa sababu shari ndio huchipuka katika ufichoni. Lakini ikiwa mazungumzo hayo ni kwa jambo la sadaka ya kuwapa watu, au kufanya jambo lolote lisio baya, au kupanga mipango ya kusuluhisha baina ya watu, hayo si mabaya. Kwani hayo ni mambo ya kheri. Na mwenye kufanya hivyo kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataa'la*, basi Mwenyezi Mungu atampa malipo makubwa duniani na Akhera.

115 Na anaye mpinga Mtume s.a.w. baada ya kwisha itambua Njia ya Haki na Uwongofu, na akaiuata njia isiyo kuwa ya Waumini, na akaingia kwenye urafiki na maadui wa Waumini, basi huyo atakuwa na hao. Kwani amekhiari kuwa hao ndio wawe marafiki zake na walenzi wake. Mwenyezi Mungu atakuja mtia Motoni Siku ya Kiyama.

116 Hakika mwisho huu wa kuumiza ni wao hao vile vile, kwani hao ni maadui wa Uislamu. Mfano wake ni mfano wa mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Hakika kila dhambi yaweza kughufiriwa, ila kumshirikisha Mwenyezi Mungu, na kumuabudu mwengine asiye kuwa Yeye, na kumpinga Mtume

117. Wao hawawaombi badala yake Yeye ila wanawake, wala hawamuombi ila Shet'ani aliye asi.¹¹⁷

118. Mwenyezi Mungu amemlaani. Naye Shet'ani alisema: Kwa yakini nitawachukua sehemu maalumu katika waja wako.¹¹⁸

119. Na hakika nitawapoteza na nitawatia matamano, na nitawaamrisha, basi watakata masikio ya wanyama, na nitawaamrisha, basi watabadili aliyo umba Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumfanya Shet'ani kuwa ni mlinzi wake badala ya Mwenyezi Mungu, basi huyo amekhasiri khasara ya dhaahiri.¹¹⁹

120. Anawaahidi na anawatia tamaa. Na Shet'ani hawaahidi ila udanganyifu.¹²⁰

121. Hao makao yao ni Jahannamu, na wala hawapati makimbilio kutoka humo.¹²¹

122. Na wale walio amini na wakatenda mema, tutawaingiza katika Bustani zipitayo mito kati yake. Watadumu humo milele. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo kweli. Na nani mkweli zaidi kwa usemi kuliko Mwenyezi Mungu.¹²²

123. Si kwa matamano yenu, wala matamano ya Watu wa Kitabu! Anaye fanya ubaya

katika Haki. Ni shani ya Mwenyezi Mungu kusamehe madhambi, ila dhambi ya kumshirikisha Yeye katika ibada. Kwa jengino lisilo kuwa hili Yeye humsamehe amtakaye. Anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu katika ibada na kumtegemea, basi huyo ameipotea Haki, na amekuwa mbali nayo mno; kwani mtu huyo ameifisidi akili yake na nafsi yake pia.

117 Katika upotovu ulio wazi kabisa ambao uko mbali na Haki ni ule wa mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Huyo anaabudu kitu ambacho hakisikii wala hakioni, hakidhuru wala hakinafishi. Na huita hiyo miungu yake kwa majina ya kike, kama Laata na Uzza na Manaata na mengineyo ya majina ya kike. Yeye hakika kwa hivyo anamuabudu Shetan.

118 Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amekwisha mfukuza huyu Shetani kutokana na kivuli cha rehema yake, na amemjaalia awe katika njia ya upotovu. Na Shetani ameapa, na amejichukulia ahadi mwenyewe, kuwa atachota miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu idadi maalumu awapumbaze kwa upotovu wake na awatie wasiwasi kwa shari yake.

119 Hakika kiapo chake Shetani ni kuwa atawapoteza wale anao wapumbaza kwa kuwatenga mbali na Haki, na kuchochea pumbao lao na matamano yao, mpaka wakawa wamepotea wanatanga tanga katika mawazo na tamaa za uwongo. Wakisha kuwa katika kuzainiwa huku na tamaa hizo chini ya utawala wake Shetani, tena huwatokomeza kwenye mambo yasiyo ingia akilini, na huwapelekea hao wafikiri kufanya hayo ni ibada. Na ilhali haya yote ni mawazo ya uwongo tu. Basi huwatia wasiwasi wakatenda mambo, kama kwa mfano kuwakata masikio baadhi ya ngamia wao, wageuze khulka aliyo iumba Mwenyezi Mungu. Wakafanya kuwa ngamia aliye katwa masikio yake hachinjwi, wala hafanyishwi kazi, wala hazuiliwi kwenda machungani atakavyo. Yote haya ni kwa amri yake Shetani kuwazaini. Tena huwatia wasiwasi mpaka wakaona kuwa hayo ni katika dini. Na hakika wao inakuwa wanamfuata yeye Shetani, na wanamfanya yeye ndiye wa kuwanusuru, na ndiye wa kumfuata badala ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumfanya Shetani ndiye msaidizi wake wa kumfuata, basi amekhasiri khasara kubwa iliyo wazi. Kwani hapo anakuwa amepotea njia ya Haki, na ameipumbaza akili yake, na utampata ufisadi duniani, na adhabu Akhera.

120 Shetani huwapambia shari, wakaiona nzuri, na huwaahidi manufaa watayo pata pindi wakitenda kitendo fulani, na huwatia katika nafsi zao matumaini ya kuyatumai. Na hapana lolote analo waahidi na analo wapambia ila ni udanganyifu mtupu.

121 Hakika hao walio zipoteza akili zao na wakafuata wasiwasi wa Shetani anao watia katika nafsi zao, mwisho wao ni kuendea Jahannamu, wala hawatapata njia ya kutoka huko.

122 Huu ndio mwisho wa wafuasi wa Shetani. Ama mwisho wa wafuasi wa Mwenyezi Mungu ni mzuri. Wao ndio walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakatenda mema, wala hawazugwi na mawazo ya uwongo. Hakika Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu Mtukufu atawatia katika mabustani yapitayo mito kati yake, chini ya vivuli. Na hayo ni makubwa mno kuliko bustani hizi za duniani. Na hayo ni yakini, kwani ahadi hizo ni ahadi za Mwenyezi Mungu, na ahadi zake haziwi ila ni hakika isiyo geuka, wala haina udanganyifu. Yeye ni mmiliki wa kila kitu. Wala haiwezi kufikirika kuwa yupo yeyote yule aliye mkweli kwa neno lake na ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu.

atalipwa kwalo, wala hatajipatia mlinzi wala wa kumnusuru, isipo kuwa Mwenyezi Mungu.¹²³

124. Na anaye fanya mema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini - basi hao wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa hata kadiri ya tundu ya kokwa ya tende.¹²⁴

125. Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule aliye usilimisha uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa mwema, na anafuata mila ya Ibrahim mwongofu? Na Mwenyezi Mungu alimfanya Ibrahim kuwa ni rafiki mwendani.¹²⁵

126. Ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo duniani. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuvizunguka vitu vyote.¹²⁶

127. Wanakuuliza nini sharia ya wanawake. Sema: Mwenyezi Mungu ana kutoleeni fatwa juu yao, na mnayo somewa humu Kitabuni kukhusu mayatima wanawake ambao hamwapi walicho andikiwa, na mnapenda kuwaoa, na kukhusu wanyonge katika watoto, na kwamba mwasimamie mayatima kwa uadilifu. Na kheri yoyote mnayo fanya Mwenyezi Mungu anaijua.¹²⁷

128. Na mwanamke akichelea kutupwa au kutojaliwa na mumewe, basi si vibaya kwao wakisikizana kwa suluhu. Na suluhu ni bora. Na nafsi zimewekewa machoni mwake tamaa na choyo. Na mkifanya wema na mkamchamngu basi hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayo yatenda.¹²⁸

123 Malipo siyo ayatamaniyo mtu na kuyaota bila ya vitendo vyema vizaavyo matunda. Malipo siyo myatamaniyo nyinyi, Waislamu. Wala siyo wayatamaniyo na kuyaota Ahlu-l-Kitabi, Watu wa Biblia, Mayahudi na Wakristo. Bali malipo na kuepukana na adhabu ni kwa Imani na Vitendo Vyema. Atendaye maovu atalipwa kwa vitendo vyake. Wala hampati mlinzi wala wa kumnusuru ila Mwenyezi Mungu.

124 Watendao mema, kwa kadiri ya uwezo wao nao wanamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wataingia kwenye Pepo ya neema, wala hawatapunguziwa hata chembe. Na hapana khitilafu baina ya malipo ya mwanamume na ya mwanamke, kwani mwanamke naye ana waajibu wake, malipo ya vitendo vyema, na adhabu kwa vitendo vibaya.

125 Msingi wa vitendo vyema ni itikadi iliyo sawa. Na bora ya dini ni kumtakasikia niya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ukawa uso wako, na akili yako, na nafsi yako, yote haitaki kitu isipo kuwa kumridhi Mwenyezi Mungu *Subhanahu*. Kwa hivyo basi ndio fahamu zako zitanyooka sawa kuufahamu ujumbe wa Mitume, na ndio utaweza kushika daima vitendo vilivyomo bora, na ukamfuata Baba wa Manabii, Ibrahim a.s. Kwani dini yake Ibrahim ndiyo Dini ya Mwenyezi Mungu, na ndiyo Dini inayo elekeza kutaka Haki daima. Na kwa Ibrahim ndiyo umekutana umoja wa Dini, kwa Waislamu, na Mayahudi na Wakristo. Basi ifuateni njia yake. Mwenyezi Mungu hakika amemkirimu Ibrahim, akamwita "Rafiki Mwendan".

126 Hakika wa kumtakasia niya ni Mwenyezi Mungu, na ndio kwake Yeye inapasa uasilimisho uso wako, yaani umuelekee na umnyenyekee. Huko ndiko kumsafia niya Mwenyezi Mungu aliye umba ulimwengu wote, na ndiye mwenye kuumiliki. Vitu vyote viliomo mbinguni na duniani - nyota, sayari, jua, mwezi, milima, mabonde, majangwa, mashamba n.k. ni vya Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mwenye kubainikiwa na kila kitu, Mwenye kujua kwa ujuzi mkamilifu wa kuvizunguka vitu vyote avitendavyo mwanaadamu. Na Yeye atamlipa kheri akitenda kheri, na shari akitenda shari.

127 Watu walimtaka Mtume s.a.w. awambie nini hukumu ya sharia juu ya wanawake. Na wanawake walikuwa, na wangali bado kuwa, ni watu wanyonge. Basi Mwenyezi Mungu amembainishia Nabii wake ili naye abainishe hali ya wanawake, na hali ya wanyonge wengine katika ukoo miongoni mwa watoto na mayatima. Na akataja kuwa mayatima wanawake ambao wanaolewa wala hawachukui mahari yao, na watoto, na mayatima, wote hao watendewe kwa uadilifu na huruma na kuraiwa. Na kwamba kila kheri itendwayo basi hakika Mwenyezi Mungu anaijua, na Yeye ndiye atakaye ilipa.

128 Na mwanamke akikhofta kuwa mumewe anapuuza mambo ya nyumbani au anayatupa, hayajali, wala hayashughuliki, basi hapana dhambi kwa wote hao wawili kutafuta njia za kusuluhiana kwa mapatano mema na kukurubiana. Na mwenye akili kati yao ni yule anaye anza kutaka masikizano. Na suluhu daima ina kheri, haina shari ndani yake. Linalo zuia masikizano ni kule kuwa kila mmoja kung'ang'ania

129. Wala hamtaweza kufanya uadilifu baina ya wake, hata mkikakamia. Kwa hivyo msimili moja kwa moja mkamwacha (mmojo) kama aliye tundikwa. Na mkisikizana na mkamchamngu basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira na Mwenye kurehemu.¹²⁹

130. Na wakitengana Mwenyezi Mungu atamtosheleza kila mmoja katika wao kwa ukunjufu wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu Mwenye hikima.¹³⁰

131. Na ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote viliomo katik mbingu na viliomo katika dunia. Na kwa hakika tuliwausia walio pewa Kitabu kabla yenu, na nyinyi pia, kwamba mumche Mwenyezi Mungu. Na mkikataa, basi ni vya Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo duniani. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, anajitoshia, na Msifiwa.¹³¹

132. Na ni vya Mwenyezi Mungu viliomo katika mbingu na viliomo katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Mlinzi.¹³²

133. Akitaka atakuondeni, enyi watu! Na awaleta wengineo. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa hayo.¹³³

134. Anaye taka malipo ya dunia, basi kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo ya dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.¹³⁴

135. Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa

haki yake kwa ukamilifu, na ugumu na uchoyo wa nafsi unapo wamiliki watu. Wala hapana njia ya kurejeza mapenzi ila mmojapo kati ya wawili kulegeza kamba. Na huyo ndiye mwema, mchamngu, mwenye kujihifadhi na dhulma. Na mwenye kutenda vitendo vyema na akamcha Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu anayo khabari ya vitendo vyake, na atamlipa kwavyo.

129 Kuwafanyia uadilifu wake kwa mapenzi ya daima yasiyo chafuliwa na udanganyifu, na kutendeana usawa katika mapenzi ikawa nipe nikupe, ni jambo lisilo wezekana kuwa. Kadhaalika haiwezi kuwepo usawa katika kuwapenda wake, ikiwa kuna zaidi kuliko mke mmoja. Walakini mkijitahidi, basi msimfanyie ujeuri mmoja wapo, mkamili upande mmoja, na mkamwacha mwengine si mke si mt'alaka. Yapasa mjitengeneze, na muendeshe nyumba zenu kwa wema si kwa ufisadi. Na mcheni Mwenyezi Mungu apate kughufrieni na akurehemuni. Ni shani yake kughufiria na kurehemu.

130 Ikiwa suluhu haikumkinika na ikawa chuki (au karaha) imeshika nguvu zaidi, basi inalazimika kufarikiana. Na wakifarikiana Mwenyezi Mungu atawatosheleza kila mmoja wao kutokana na ukunjufu wa rehema yake na fadhila yake. Na riziki ziko katika mikono ya Mwenyezi Mungu, na Yeye ndiye Mwenye hikima, na hupanga mambo yote kwa mipango yake.

131 Kiini cha Dini ni kumnyenyekea Mwenye kuumba ulimwengu, Mwenye utukufu na ukarimu, na kuukubali ufalme wake usio na ukomo. Kwani ni vya Mwenyezi Mungu vyote viliomo mbinguni na katika ardhi. Na kwa huu Ufalme usio na ukomo amesema: Tumewausia watu wa dini zilizo toka mbinguni, katika Watu wa Kitabu na nyinyi Waislamu, mumkhofu Mwenyezi Mungu, na mumuabudu Yeye, na msiwe mnakufuru katika ibada yake, maana Yeye ndiye Mwenye utawala mkubwa kushinda wote. Hapana kitu kilicho toka nje ya utawala wake. Yeye ni Mkwasi, yaani mwenye kujitoshia wala hakuhitajiini nyinyi. Juu ya hivyo Yeye anakuhimidini kwa imani yenu, kwani kwa kuwa Yeye ni Mwenye kujitosheleza mwenyewe, juu ya hivyo anasifu na kushukuru vitendo vyema vya waja wake.

132 Kupanga kila kitu cha mbinguni na duniani ni kazi ya Mwenyezi Mungu Aliye takasika na Aliye tukuka. Yeye ndiye Mwenye madaraka, Mwenye kuendesha, Mwenye kupanga. Yatosha kuwa Yeye ndiye Mtawala aliyehamrisha ulimwengu ukajipanga ulivyo jipanga, na akawaamrisha watu wamuabudu, na wamtegemezee Yeye mambo yao, na wamche Yeye.

133 Hakika nyinyi enyi waja wa Mwenyezi Mungu! Mko chini ya ufalme wa Mwenyezi Mungu Mwenye uweza na Mwenye nguvu. Akipenda atakufisheni na alete wengine kabisa. Na Yeye Mwingi wa Utukufu ni Muweza wa hayo, na Muweza wa kila kitu.

134 Na watu, pindi wakitafuta neema za dunia zilizo halali kwa njia ya haki iliyo nyooka sawa, basi hakika Mwenyezi Mungu atawapa neema za duniani na Akhera; kwani Yeye ndiye aliyehamrisha neema zote mbili.

ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu, au wazazi wawili na jamaa zenu. Akiwa tajiri au masikini Mwenyezi Mungu anawastahikia zaidi. Basi msifuuate matamano, mkaacha kufanya uadilifu. Na mkiupotoa au mkajitenga nao basi Mwenyezi Mungu anajua vyema mnayo yatenda.¹³⁵

136. Enyi mlio amini! Muaminini Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Kitabu alichokiteremsha juu ya Mtume wake, na Kitabu alichokiteremsha kabla yake. Na anaye mkataa Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya Akhera, basi huyo amekwisha potelea mbali.¹³⁶

137. Hakika walio amini, kisha wakakufuru, kisha wakaamini, kisha wakazidi ukafiri, Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaghufiria wala wa kuwaongoa njia.¹³⁷

138. Wabashirie wanaafiki kwamba watapata adhabu chungu,¹³⁸

139. Wale ambao huwafanya makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je! Wanataka wapate kwao utukufu? Basi hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu.¹³⁹

140. Naye amekwisha kuteremshieni katika Kitabu hiki ya kwamba mnapo sikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakanushwa na zinafanyiwa kejeli, basi msikae pamoja nao, mpaka waingie katika mazungumzo mengine. Hivyo mtakuwa nanyi mfano wao hao. Hakika Mwenyezi Mungu atawakusanya wanaafiki na makafiri wote pamoja katika Jahannamu,¹⁴⁰

135 Uadilifu ndio nidhamu ya maumbile. Na hiyo ndiyo sharia ambayo haiwezi kuwapo ndani yake maoni ya kukhitalifiana. Basi enyi mlio mt'ii Mwenyezi Mungu wa Haki, na wito wa Mitume wake, kuweni macho nafsi zenu katika kuut'ii uadilifu, na kuweni macho kwa ajili ya watu. Mfanyieni insafu aliye dhulumiwa, na msimame imara, si kwa ajili ya kumpendelea tajiri, au kumwonea huruma masikini. Kwani Mwenyezi Mungu aliye waumba matajiri na masikini anastahiki zaidi kuangalia hali ya tajiri au fakiri. Matamano ndiyo yanayo mpelekea mtu kumili nafsi yake, basi msiyafuate matamano mkaacha uadilifu. Na mkikengeuka mkaacha uadilifu, au mkapuza kusimamisha uadilifu, basi mjue Mwenyezi Mungu anayajua myatendayo, tena anayajua kwa ujuzi wa ndani. Naye atakulipeni kwa mujibu wa a'mali yenu; ikiwa njema mtalipwa wema, ikiwa ovu mtalipwa shari.

136 Kwa hakika Ujumbe wa mbinguni ni mmoja, kwa kuwa yule Mwenye kutuma ni Mmoja, naye ni Mwenyezi Mungu. Basi enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu na mumsafie niya. Na msadikini Mtume wake Muhammad, na msadiki yaliyo kuja katika Kitabu chake alichokiteremshia, na mtende yaliyo amrishwa humo. Na sadikini Vitabu vilivyoteremshwa kabla yake kama alivyo teremsha Mwenyezi Mungu bila ya mageuzo wala kusahau. Aminini yote hayo. Kwani mwenye kumkanusha Mwenyezi Mungu, Muumba wa viumbe vyote, na Malaika, na Mwenye kuyajua yaliyo fichikana, na Vitabu vya Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na akaikanusha Siku ya Mwisho, basi huyo ameipotea Njia Iliyo Nyooka, na ametokomea mbali katika njia ya upotovu.

137 Hakika Imani ni kuit'ii Haki kusio kuwa na ukomo, na kunako endelea daima. Basi wanao taradadi wakababaika si Waumini. Hao ambao wanaamini, kisha wakakufuru, kisha wakaamini, kisha wakakufuru, na kwa hivyo wakazidi ukafiri wao - Mwenyezi Mungu hatakuwa wa kuwaghufiria watu hao hivyo vitendo vyao viovu, wala hatawaongoa kwenye Haki. Kwani kusamehe kwa Mwenyezi Mungu kunahitajia toba, na kujing'oa na shari, na uwongofu wake ni kwa wale wanao ileleka Haki na wanaitaka.

138 Ewe Mtume Mtukufu! Waonye wanaafiki kwamba Siku ya Kiyama watapata adhabu chungu yenye kuumiza.

139 Hao wanaafiki huufanya utawala wa makafiri uwe juu yao, na wanawawacha Waumini. Basi hebu hivyo wanataka wapate utukufu kwa hawa makafiri? Hakika utukufu uko kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Yeye huwapa waja wake wenye kuamini. Na mwenye kutaka utukufu kwa Mwenyezi Mungu atakuka, na mwenye kutaka utukufu kwa mwinginewe atadhalilika.

140 Mwenyezi Mungu amekwisha kuteremshieni katika Qur'ani Tukufu kwamba kila mkisikia Aya za Kitabu nyinyi mnaamini, na makafiri wanapinga na wanakejeli. Na ikiwa hivyo ndiyo hali ya makafiri na wanaafiki, na mkasikia kejeli zao, basi msikae nao, mpaka waingie katika mazungumzo mengine waache dhihaki zao. Na nyinyi ikiwa hamtofanya hivyo, mkawa mnasikiliza kejeli zao, basi mtakuwa

141. Wale ambao wanakungojeeni, mkipata ushindi unao toka kwa Mwenyezi Mungu wao husema: Si tulikuwa pamoja nanyi vile? Na ikiwa ni sehemu ya makafiri kushinda wao huwaambia: Hatukuwa ni waweza wa kukushindeni, nasi tukakuingeni na hawa Waumini? Basi Mwenyezi Mungu atahukumu baina yenu Siku ya Kiyama, wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini.¹⁴¹

142. Hakika wanaafiki wanamkhadaa Mwenyezi Mungu, na hali ni Yeye ndiye mwenye kuwakhadaa wao. Na wanapo inuka kusali huinuka kwa unyong'onyo, wanajionyesha kwa watu tu, wala hawamdhukuru Mwenyezi Mungu ila kidogo tu.¹⁴²

143. Wanayumba yumba baina ya huku na huko. Huku hawako na huko hawako. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha kupotea, kabisa hutompatia njia.¹⁴³

144. Enyi mlio amini! Msiwafanye makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je, mnataka Mwenyezi Mungu awe na hoja iliyo wazi juu yenu?¹⁴⁴

145. Hakika wanaafiki watakuwa katika t'abaka ya chini kabisa Motoni, wala hutompata yeyote wa kuwanusuru.¹⁴⁵

146. Isipo kuwa wale walio tubu, na wakatengeneza na wakashikamana na Mwenyezi Mungu, na wakamtakasia Dini yao Mwenyezi Mungu. Basi hao ni pamoja na Waumini. Na Mwenyezi Mungu atakuja wapa Waumini ujira mkubwa.¹⁴⁶

nanyi kama wao katika kuifanyia maskhara Qur'ani. Mwisho wa makafiri na wanaafiki ni muovu mno, kwani Mwenyezi Mungu atawakusanya wote hao katika Moto wa Siku ya Kiyama.

141 Mtindo wa wanaafiki ni kukungojeeni kama anavyo ngojea mwenye husda na maya anaye tamani mpate masaibu mnapo kuwa katika vita na maadui. Mkishinda kwa nusra ya Mwenyezi Mungu, na mkafungukiwa njia ya Haki, wao huwaambia Waumini - na hali wao ule ushindi walio pewa wenye Imani na Mwenyezi Mungu umewashtusha : Sisi hatukuwa nanyi? Kwa maana sisi ni jamaa zenu! Na ikiwa ni zamu ya makafiri kupata ushindi, basi wao huwaendea na kuwaambia: Sisi hatukuyashughulikia mambo yenu hata yakawa ni yetu? Na hatukukupeni mapenzi yetu, na tukakulindeni na hawa Waumini? (yaani sisi ni wenzenu). Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* atakuhukumuni baina yenu na hawa wanaafiki Siku ya Kiyama. Wala Mwenyezi Mungu hatowapa makafiri njia kuwashinda Waumini maadamu Waumini watashikamana na sifa ya Imani ya kweli na vitendo vyema.

142 Hakika wanaafiki, kwa ule unaafiki wao, wanadhani kuwa wanamkhadaa Mwenyezi Mungu Mtukufu na wanamficha hakika ya nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni Yeye ndiye anaye wakhadaa wao. Basi Yeye huwapururia kuwapa muhula, na anawawacha mpaka wabobee katika maovu yao, kisha ndio awahisabu kwa walio yatenda. Na hawa wanaafiki wana dhaahiri ya kuonekana, na ya ndani ya nafsi zao. Yale ya kuonekana ni vile kuwa wakiinuka kwenda kusali huinuka kwa uvivu, kwa unyong'onyo. Na sala yao ni riya tu, kuonyesha, si ya kweli. Na ya ndani ni kuwa hawakumbuki kumtaja Mwenyezi Mungu ila kwa nadra, kwa tukizi. Na lau kuwa wanamkumbuka vilivyo wangeli uacha unaafiki.

143 Na hawa wanaafiki ni watu wanao taradadi, wanababaika. Kwenu hawapo, na kwao makafiri hawapo katika kila hali. Na hayo ni kwa sababu ya udhaifu wa imani, na udhaifu wa nafsi, na kwa sababu ya kupotoka na Haki. Na mwenye kuandikiwa kupotoka na Mwenyezi Mungu tangu hapo azali, basi huna njia wewe ya kumwongoa sawa.

144 Hakika katika sababu za unaafiki ni kuwa wanaafiki wamewafanya watu wasio kuwa Waumini kuwa ndio walenzi wao, marafiki zao, watawala wao, na ndio wa kuwanusuru. Enyi Waumini! Yaacheni haya, muepukane nayo. Wala msiwafanye makafiri ndio wa kukunusuruni, wakukutawalini, mkawanyenyekae. Na hapana shaka yoyote mkifanya hivyo mnampa Mwenyezi Mungu hoja iliyo wazi ya kukuhojini. Mtakuja ingia pamoja na wanaafiki, na mtadhalilika. Kwani inakuwa hamfanyi utukufu wenu utoke kwa Mwenyezi Mungu, na kwa haki, na vitendo vyema.

145 Hakika wanaafiki kwa sababu ya unaafiki wao watakuwa katika vina vya Jahannamu. Wao wako chini kabisa huko, na daraja ya mwisho kabisa. Wala hutompata wa kuwanusuru, wa kuwatetea na adhabu hiyo.

146 Isipo kuwa wale katika wao walio tubia, na wakarejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na wakaungana naye Yeye peke yake, na wakajitakasa, na wakaelekeza nyuso zao kwake, na wakatenda

147. Mwenyezi Mungu hakuadhibuni mkimshukuru na mkamuamini. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kupokea shukrani na ndiye Mwenye kujua.¹⁴⁷

148. MWENYEZI MUNGU hapendi uovu uenezwe kwa maneno ila kwa mwenye kudhulumiwa. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.¹⁴⁸

149. Mkidhihirisha wema au mkiuficha, au mkiyasamehe maovu, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira na Muweza.¹⁴⁹

150. Hakika wale wanao mkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wanataka kufarikisha baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume wake, kwa kusema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa. Na wanataka kushika njia iliyo kati kati ya haya,¹⁵⁰

151. Hao ndio makafiri kweli. Na tumewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha.¹⁵¹

152. Na walio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, wala wasimfarikishe yeyote kati yao, hao atawapa ujira wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, na Mwenye kurehemu.¹⁵²

153. Watu wa Kitabu wanakutaka uwateremshia kitabu kutoka mbinguni. Na kwa hakika walikwisha mtaka Musa makubwa kuliko hayo. Walisema: Tuonyeshe Mwenyezi Mungu wazi wazi. Wakapigwa na radi kwa hiyo dhulma yao. Kisha wakamchukua ndama kumuabudu, baada ya kwisha wajia hoja zilizo wazi. Nasi tukasamehe hayo, na tukampa Musa nguvu zilizo dhaahiri.¹⁵³

mema. Wakifanya haya basi ndio wanakuwa miongoni mwa Waumini. Watapata malipo ya Waumini. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amekwisha waahidi Waumini malipo makubwa duniani na Akhera.

147 Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hana alitakalo kwenu ila mumuamini Yeye, na muishukuru neema yake. Mkiwa hivyo basi hampati adhabu, bali mtapata malipo ya kheri na shukrani. Kwani hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mwenye kushukuria waja wake kwa vitendo vyema, na ni Mjuzi, anajua hali zao zote njema na mbaya.

148 Mwenyezi Mungu anawakataza waja wake wasiseme maneno maovu, ila yule aliye patwa na dhulma. Ni halali kwake kumshitaki aliye mdhulumu, na autaje uovu aliyo tendewa. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni Mwenye kusikia vyema maneno ya aliye dhulumiwa. Na ni Mjuzi wa dhulma ya mwenye kudhulumu. Na atamlipa kwa kitendo chake hicho.

149 Mkiyadhihirisha mema myatendayo, au mkayaficha, au mkamsamehe anaye kufanyieni uovu, Mwenyezi Mungu atakulipeni kwa kufuata khulka yake Mtukufu, ya kusamehe na hali ana uwezo kaamili. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni mwingi mno wa kusamehe, Mwenye kukamilika uwezo wake.

150 Hakika wasio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wanao taka kufanya ubaguzi katika imani ya Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wanasema: Tunawaamini baadhi ya Mitume, sio wote, hao wanawaamini wapapendao na wanawakataa wasio wapenda. Na lilio waajibu ni kuwaamini wote, kwani Imani haikubali kukatwa mapande mapande.

151 Hawa wote ndio walio ungama ukafiri wao ulio wazi. Na Mwenyezi Mungu amekwisha waahidi wao na mifano ya hao adhabu kali yenye kudhalilisha.

152 Na ama wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, wala hawakumkanusha hata mmoja wapo kati yao, basi hapana shaka Mwenyezi Mungu atawalipa malipo makubwa kwa ajili ya Imani yao iliyo kamilika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira kwa wenye kutubu, na ni Mwenye kuwarehemu waja wake.

153 Ewe Mtume! Watu wa Kitabu, yaani Mayahudi wapendao kuudhi, wanakutaka ulete dalili ya ukweli wa unabii wako. Uwalettee kitabu mahksusi kiwateremkie kutoka mbinguni kithibitishe ukweli wa utume wako, na kiwatake wakuamini na kukut'ii! Ukiyaona makuu hayo wayatakayo, wewe usifanye haraka. Kwani wenzao walio tangulia walifanya kero vile vile, wakamtaka Musa makubwa kuliko hayo. Walimwambia: Tuonyeshe Mwenyezi Mungu tumwone kwa macho. Mwenyezi Mungu akawaadhibu kwa lile kero lao na dhulma yao kwa kuwapiga radi iliyo wateketeza!! Kisha watajije hawa watu kosa kubwa zaidi na ovu zaidi, nalo ni pale walipo mfanya ndama kuwa ni mungu wao, wakamwacha Mwenyezi Mungu aliye waumba. Haya baada ya kwisha ona dalili zote alizo zionyesha Musa kwa Firauni na kaumu

154. Na tukanyanyua mlima juu yao kwa kufanya agano nao. Na tukawaambia: Ingilieni mlangoni kwa unyenyekevu. Na tukawaambia: Msiivunje Siku ya Sabato (Jumaa mosi). Na tukachukua kwao ahadi iliyo madhubuti.¹⁵⁴

155. Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi zao, na kuzikataa kwao ishara za Mwenyezi Mungu, na kuwauwa kwao Manabii bila ya haki, na kusema kwao: Nyoyo zetu zimefumbwa; bali Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri kwa kufuru zao, basi hawaamini ila kidogo tu.¹⁵⁵

156. Na pia kwa kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa,¹⁵⁶

157. Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuwa wala hawakumsalibu, bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuwa kwa yakini.¹⁵⁷

158. Bali Mwenyezi Mungu alim- tukuza kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹⁵⁸

159. Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.¹⁵⁹

yake!! Kisha juu ya hayo Mwenyezi Mungu akawakunjulia usamehevu wake kwao, na Mwenyezi Mungu akampa nguvu Musa kwa hoja zilizo wazi, na neno madhubuti.

154 Mwenyezi Mungu akaunyanyua mlima juu ya Wana wa Israili ili kuwatisha kwa kule kuikataa kwao sharia ya Taurati, mpaka wakaikubali. Akachukua kwao agano, na akawaamrisha waingie mjini hali wakimnyenyekea Mwenyezi Mungu. Wala wasiyakiuke aliyo waamrisha kushika ibada katika siku ya Sabato, yaani Jumaamosi. (Imeitwa “Sabt” Kiarabu, “Shabbath” Kiyahudi, “Sabbath” Kiingereza, na “Sabato” Kiswahili, maana yake “Mapumziko” kwa kuwa ni siku ya mapumziko kwa Mayahudi.) Na Mwenyezi Mungu alichukua kwao ahadi ya nguvu.

155 Mwenyezi Mungu akawakasirikia kwa sababu ya kuvunja agano hili, na kuzikataa ishara za Mwenyezi Mungu, na kwa kuwauwa Manabii kwa dhulma, na kuendelea katika upotovu wao kwa kusema: Nyoyo zetu zimefungwa hazikubali hayo unayo tuitia! Nao hawasemi kweli katika kauli yao hiyo, bali Mwenyezi Mungu amezifuta nyoyo zao kwa ukafiri wao, basi ni wachache tu kati yao wanao amini.

156 Na Mwenyezi Mungu amewaghadhibikia Mayahudi kwa sababu ya kufuru yao na kumzulia Maryam uzushi mkubwa.

157 Na Mwenyezi Mungu pia amewaghadhibikia kwa kusema kwao uwongo: Hakika sisi tumemuuwa Masihi Isa bin Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na kweli ya yakini ni kuwa hawakumuwa kama wanavyo zua. Wala hawakumsalibu kama wanavyo dai. Lakini walifananishiwa, nao wakadhani kuwa wamemuuwa na wamemsalibu. Na hakika walimuuwa na kumsalibu aliye shabihiana naye. Nao wakaja kukhitalifiana baada ya hayo, kuwa aliyeuwawa ni Isa au mtu mwengine? Na wote hao, kwa hakika, wamo katika shaka tu juu ya jambo hilo. Kweli iliyopo ni kuwa hawana ujuzi nayo mambo haya, ila ni dhana dhana tu. Kabisa hawakumuwa Isa. (Wataalamu wa Biblia mpaka hii leo wamo kuzozana katika jambo hili. Mwenye kuzichungua Injili zinazo kubaliwa na Wakristo ataona kuwa hazina uthibitisho kuwa aliye salibiwa ndiye Yesu, au hata huyo naye alikufa msalabani au la.)

158 Bali Mwenyezi Mungu alimtukuza kwake, akamwoko na maadui zake, wasimsalibu na wasimuuwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushinda, hashindikiki, ni Mwenye hikima katika vitendo vyake. (Taurati inayo kubaliwa na Mayahudi na Wakristo imesema kuwa anaye kufa kwa kutundikwa msalabani amelaaniwa. Ndio maana Mayahudi wakawa na hamu wamtundike Nabii Isa ili wathibitisho kuwa huyo si chochote ila ni mlaanifu. Je, Mwenyezi Mungu Mtukufu vipi aachilie jambo hilo liwe kwa Mtume wake?).

159 Na hapana mmojapo katika Watu wa Kitabu (Mayahudi na Wakristo) ila atakuja tambua uhakika wa Isa (kuwa ni Nabii wa kweli wa Mwenyezi Mungu, si mwana haramu, wala si mwana wa Mungu) kabla ya kufa kwake, na kuwa yeye Isa ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na atakuja amini imani ambayo haitomfaa kitu, kwa kuwa wakati wake umekwisha pita. Na Siku ya Kiyama Isa atatoa ushahidi juu yao kuwa yeye alifikisha ujumbe, na kuwa yeye ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

- 160.** Basi kwa dhulma yao Mayahudi tuliwahirimishia vitu vizuri walivyo halalishiwa. Na kwa sababu ya kuwazuilia kwao watu wengi na Njia ya Mwenyezi Mungu,¹⁶⁰
- 161.** Na kuchukua kwao riba, nao wamekatazwa, na kula kwao mali ya watu kwa dhulma. Basi tumewaandalia makafiri katika wao adhabu yenye uchungu.¹⁶¹
- 162.** Lakini walio bobea katika ilimu miongoni mwao, na Waumini, wanayaamini uliyo teremshiwa wewe, na yaliyo teremshwa kabla yako. Na wanao shika Sala, na wakatoa Zaka, na wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho - hao tutawapa malipo makubwa.¹⁶²
- 163.** Hakika Sisi tumekuletea wahyi wewe kama tulivyo wapelekea wahyi Nuhu na Manabii walio kuwa baada yake. Na tulimpelekea wahyi Ibrahim na Ismail na Is-haka na Yaakub na wajukuu zake, na Isa na Ayub na Yunus na Harun na Suleiman, na Daud tukampa Zaburi.¹⁶³
- 164.** Na Mitume tulio kwisha kukuhadithia kabla yake, na Mitume wengine hatukukuhadithia. Na Mwenyezi Mungu alinena na Musa kwa maneno.¹⁶⁴
- 165.** Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹⁶⁵
- 166.** Lakini Mwenyezi Mungu anayashuhudia aliyokuteremshia wewe. Ameyateremsha kwa kujua kwake - na Malaika pia wanashuhudia. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.¹⁶⁶
- 167.** Hakika walio kufuru na wakazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu, wamekwisha

160 Kwa sababu ya udhalimu wao Mayahudi Mwenyezi Mungu amewapa adabu - amewakataza vyakula mbali mbali vilivyo vizuri, vimekuwa kwao haramu, na ilhali kwanza vilikuwa halali kwao. Na kwa udhalimu wao wamewazuia watu wengi wasiingie katika Dini ya Mwenyezi Mungu.

161 Na kwa sababu ya kupenda kula riba - na Mwenyezi Mungu alikwisha wakataza hayo - na kuchukua mali ya watu kwa njia isiyo ya haki, ndio ikawa adabu ya dini ni kuwazuilia na kula vyakula vilivyo vizuri. Na Mwenyezi Mungu amewawekea hao walio kufuru adhabu yenye kutia machungu.

162 Lakini walio bobea katika ilimu, yaani wataalamu kweli kweli, miongoni mwa Mayahudi, na Waumini katika umma wako, ewe Nabii, wanasadiki wahyi ulio funuliwa wewe, na walio letewa Mitume wa kabla yako. Na wanao shika Sala baraabara, na wanatoa Zaka, na wanamuamini Mwenyezi Mungu na kufufuliwa na hisabu, hao Mwenyezi Mungu atawalipa malipo mema kabisa kwa imani yao na ut'iifu wao.

163 Hakika Sisi tumekufunulia wewe, ewe Nabii! (tumekuteremshia Wahyi), Qur'ani na Sharia, kama tulivyo wafunulia kabla yako Nuhu na Manabii wa baada yake, na kama tulivyo wapa Wahyi Ibrahim, na Ismail, na Is-haq, na Yaakub, na wajukuu zake, nao wale walio kuwa Manabii wa Mwenyezi Mungu miongoni mwa dhuriya (wazao) wa Yaakub, na Isa, na Ayubu, na Yunus, na Haaran, na Suleiman, na kama tulivyo mfunulia Daud tukamteremshia Kitabu cha Zabur.

164 Kadhaalika tumewatuma Mitume wengi ambao tumekwisha taja khabari zao kabla yake. Na Mitume wengine hatukukusimulia hadithi zao. Na njia ya kumpa Wahyi Musa ilikuwa Mwenyezi Mungu akisema naye moja kwa moja nyuma ya pazia, lakini bila ya kuwepo mwengine kati.

165 Tuliwapeleka Mitume hao kuwapa bishara njema ya thawabu wenye kuamini, na kuwaonya adhabu wale walio kufuru, ili watu wasiwe na hoja ya kumtafutia kisababu Mwenyezi Mungu baada ya kwisha wapeleka Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu, ni Mshindi, wala hana yeyote madaraka pamoja naye, na ni Mwenye hikima kwa atendayo.

166 Lakini ikiwa hao watu hawashuhudii kukusadikisha, basi Mwenyezi Mungu Mwenyewe anashuhudia kuwa aliyokuteremshia ni sahihi. Hakika Yeye amekuteremshia hayo kwa hikima, na kwa mujibu wa ujuzi wake. Na Malaika nao wanashuhudia hayo kadhaalika. Na ewe Mtume! Yakutosha wewe ushahidi wa Mwenyezi Mungu, kuliko ushahidi wowote mwengine.

potelea mbali.¹⁶⁷

168. Hakika wale walio kufuru na wakadhulumu hawi Mwenyezi Mungu kuwasamehe wala kuwaongoa njia.¹⁶⁸

169. Isipo kuwa njia ya Jahannamu. Humo watadumu milele. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.¹⁶⁹

170. Enyi Watu! Amekwisha kujieni Mtume huyu na haki itokayo kwa Mola wenu Mlezi. Basi aminini, ndiyo kheri yenu. Na mkikakanusha basi hakika viliomo mbinguni na duniani ni vya Mwenyezi Mungu tu. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.¹⁷⁰

171. Enyi Watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msimseme Mwenyezi Mungu ila kwa lilio kweli. Hakika Masihi Isa mwana wa Maryamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na neno lake tu alilo mpelekea Maryamu, na ni roho iliyo toka kwake. Basi Muaminini Mwenyezi Mungu na Mitume wake. Wala msiseme: Utatu. Komeni! Itakuwa kheri kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu mmoja tu. Ametukuka Yeye na kuwa na mwana. Ni vyake Yeye vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mtegemewa wa kutosha.¹⁷¹

172. Masihi hataona uvunjifu kuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu, wala Malaika walio karibishwa. Na watakao ona uvunjifu utumwa wa Mwenyezi Mungu na kufanya

167 Hakika wale ambao wamekufuru wasikusadiki wewe, na wakawazulia watu wasiingie katika Dini ya Mwenyezi Mungu, bila ya shaka wamekuwa mbali mno na Haki.

168 Wale walio kufuru, na wakajidhulumu nafsi zao, na wakamdhulumu Mtume kwa kuupinga ujumbe wake, na wakawadhulumu watu walipo wafichia Haki, Mwenyezi Mungu hatowasamehe kamwe maadamu watabaki katika ukafiri wao. Wala hatawapa uwongofu wa kuijua njia ya kuvuka. Sio mtindo wake Subhanahu kuwasamehe watu kama hao nao wangali kubaki katika upotovu wao.

169 Lakini atawapeleka kwenye njia ya Motoni, na humo wabakie daima dawamu. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu ni jambo jepesi.

170 Enyi watu! Amekwisha kukujieni Mtume huyu, Muhammad, na Dini ya Haki kutokana na Mola Mlezi wenu. Basi yaaminini alipo kuja nayo; ndiyo itakuwa kheri yenu. Na pindi mkikataa ila kukufuru tu, basi mjue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkwasi na imani yenu, hana haja nayo. Yeye ndiye Mwenye kukumilikini nyinyi. Kwani vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi ni vyake Yeye, kwa kuvimiliki, kuviumba na kuvendesha atakavyo. Naye ni Mwenye kuvijua vyema viumbe vyake, ni Mwenye hikima katika uendeshaji wake. Hauptotezi ujira wa mwema, wala hapuuzi kumlipa mwovu.

171 Enyi Watu wa Kitabu! Msipindukie haki, mkazidisha kupita kiasi katika dini yenu, wala msimzulia uwongo Mwenyezi Mungu, mkaukanya utume wa Isa, au mkamfanya kuwa ni Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu. Kwani Masihi ni Mtume kama walivyo Mitume wengine. Mwenyezi Mungu amemuumba kwa uwezo wake na neno lake alilo mbashiria kwalo, na Jibrili akampulizia Maryamu roho ya Mwenyezi Mungu. Hii ni siri katika siri za uwezo wake Mwenyezi Mungu. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mitume wake wote imani ya kweli. Wala msidai kuwa katika Ungu kuna Utatu!! Tokeni katika upotovu huu, itakuwa kheri kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu mmoja tu, wala hana mshirika wake. Naye ametakasika na kuwa na mwana! Na kila kilioko katika mbingu na ardhi ni chake. Na Yeye Mwenyewe anajitoshia peke kuwa ni Mwendeshaji wa Ufalme wake. (Kuitwa Nabii Isa Neno au Roho iliyo toka kwa Mungu, hakupi Ungu. Yeye ni neno kwa kuumbwa kwa amri ya “Kun”, “Kuwa” akawa. Haya ni kuwapinga Mayahudi walio dai kuwa yeye ni mwanaharamu. Basi wanaambiwa kuwa ameumbwa kama vilivyo umbwa vitu vyote, kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Naye ni Roho iliyo toka kwa Mwenyezi Mungu kama walivyo pewa Waumini wote (58.22) na alivyo puliziwa Adam (15.29) na kwa hivyo wanaadamu wote (32.7-9). Hapana hata pahala pamoja katika Injili ziliomo katika Biblia ambapo Yesu (Nabii Isa a.s.) alijiita mwenyewe Mwana wa Mungu. Kila mara akijiita Mwana wa Adamu. Na alipo mwita Mungu Baba, alikusudia ni Baba wa watu wote, kama alipo sema: “Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu.” Injili ya Yohana 10.33-36.)

kiburi, basi atawakusanya wote kwake.¹⁷²

173. Na ama walio amini na wakatenda mema atawalipa ujira wao sawa sawa, na atawazidishia kwa fadhila yake. Na ama wale walio ona uvunjifu na wakafanya kiburi, basi atawaadhibu adhabu iliyo chungu. Wala hawatopata mlinzi wala wa kuwanusuru asiye kuwa Mwenyezi Mungu.¹⁷³

174. Enyi watu! Umekufikieni ushahidi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Na tumekuteremshieni Nuru iliyo wazi.¹⁷⁴

175. Ama wale walio muamini Mwenyezi Mungu, na wakashikamana naye, basi atawatia katika rehema yake na fadhila, na atawaongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka.¹⁷⁵

176. Wanakuomba uhukumu, sema: Mwenyezi Mungu anakupeni hukumu juu ya mkiwa. Ikiwa mtu amekufa, naye hana mtoto, lakini anaye ndugu wa kike, basi huyo atapata nusu alichu acha maiti. Na mwanamume atamrithi ndugu wa kike ikiwa hana mwana. Na ikiwa wao ni ndugu wa kike wawili, basi watapata thuluthi mbili za alichu acha maiti. Na wakiwa ndugu wanaume na wanawake, basi mwanamume atapata sehemu iliyo sawa na ya wanawake wawili. Mwenyezi Mungu anakubainishieni ili msipotee; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.¹⁷⁶

172 Masihi hakujiona bora hata akatae kuwa ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu, wala hawakujiona bora Malaika walio karibishwa. Na mwenye kutakabari na kujiona mtu wa juu hataweza kuikimbia adhabu ya Mwenyezi Mungu Siku atakayo wakusanya watu kwa ajili ya hisabu.

173 Ama walio amini wakatenda mema atawalipa thawabu za vitendo vyao, na atawazidishia kwa fadhila yake, kwa kuwakirimu na kuwaneemesha. Na ama wale walio kataa kumuabudu, na wakajiona bora wasimshukuru, hao amewaandalia adhabu yenye machungu makali. Hapana msaidizi wa kuwakinga nayo wala wa kuwanusuru.

174 Enyi watu wote! Zimekwisha kujieni dalili zilizo wazi za ukweli wa Mtume Muhammad. Na tumekuteremshieni kwa ulimi wake Qur'ani iliyo wazi kama mwangaza, unao angaza Njia, na inayo kuongozeni kwendea mafanikio.

175 Ama walio msadiki Mwenyezi Mungu na ujumbe wake alio leta, na wakaifuata Dini yake, atawatia katika Bustani zake Akhera, na atawamiminia rehema yake, na atawakusanya katika ukunjufu wa fadhila yake, na atawawezesha hapa duniani kuthibiti katika Njia yake Iliyo Nyooka.

176 Ewe Nabii! Wanakuuliza vipi atarithiwa aliye kufa naye akawa hana mwana, wala mzazi. Sema: Hakika hukumu ya Mwenyezi Mungu katika urithi wa hawa ni kuwa, akiwa maiti ana ndugu wa kike basi atapata nusu ya mali. Na akiwa maiti ni mwanamke naye ana ndugu wa kiume basi atarithi mali yote. Na ikiwa ameacha ndugu wawili wa kike, basi watapata hao thuluthi mbili ya urithi. Na ikiwa hao ndugu ni mchanganyiko wanaume na wanawake, basi fungu la mwanamume ni sawa na mafungu mawili ya wanawake. Mwenyezi Mungu anakubainishieni haya msije mkapotea katika kugawa mafungu ya urithi. Na Mwenyezi Mungu ni Mkamilifu wa ujuzi wa a'mali zenu na vitendo vyenu vyote. Na atakulipeni kwavyo. (Angalia: Urithi wa ndugu katika Aya hii ni wa ndugu khalisa, yaani ndugu kwa baba na mama, au ndugu kwa baba. Ama urithi wa ndugu kwa mama tu umekwisha tajwa katika Aya 12 ya Sura hii ya An-Nisaa). (*Tazama Maelezo 4:176*)

Sura 5 - Al-Maida

Utangulizi

Hii Sura ya Madina. Idadi za Aya zake ni 120. Na hii ni katika Sura zilizo shuka karibu na mwisho. Humu umebainishwa waajibu wa kutimiza maagano, sawa yakiwa baina ya mja na Mola wake Mlezi, au baina ya watu wenyewe kwa wenyewe. Na Sura hii imebainisha baadhi ya vyakula vilivyo harimishwa, kama ilivyo bainisha vilivyo halali, na kuhalalisha kuwaoa wanawake wa Ahlil Kitabi, Wakristo na Mayahudi. Zimetajwa pia humu nguzo za udhu na kutayamamu. Kadhaalika imeelezwa kutakikana kufanya uadilifu na adui. Na Sura hii imeashiria neema za Mwenyezi Mungu juu ya Waislamu, na waajibu wao kukihifadhi Kitabu chao, na ikaelezea kuwa Mayahudi wameyatengua maneno kutokana na pahala pake, na Wakristo wakayasahau baadhi ya mambo waliyo kumbushwa, na kwamba wao wamekufuru kwa kusema kwao kuwa Masihi ni mwana wa Mungu. Kadhaalika Sura hii inawakanusha Mayahudi na Wakristo kwa yale madai yao kwamba ati wao ni wana wa Mungu na vipenzi vyake. Kisha tena Sura hii imekusanya baadhi ya khabari za Mayahudi, kama ilivyo kusanya kisa cha wana wawili wa Adam. Kisa hichi kinathibitisha kuwa uvamizi na kudhulumiana ni katika tabia za kibinaadamu. Tena kuwajibika kumtoza kisasi mwenye kudhulumu ni njia ya kuidhibiti tabia hii mbovu isivuke mpaka! Na Sura Al Maidah imeeleza adhabu ya kumtia adabu mwenye kufanya fiski na wizi. Tena baadae ikarejea kubainisha vipi Mayahudi walivyo pindua hukumu za sharia zilizo kuwamo katika Taurati, na ikabainisha kwamba katika Taurati na Injili ulikuwapo ukweli na haki kabla ya kuchezeza na kugeuzwa geuzwa. Na ikahakikishwa kuwa ni waajibu kuhukumu kwa mujibu alivyo teremsha Mwenyezi Mungu. Sura imeashiria juu ya uadui wa Mayahudi na Wakristo kwa Waumini, na waajibu wa kutowanyenyekea, na kutowaridhia kwa wanayo tenda, na kuwa ni dharura kuwapinga. Na Sura imethibitisha kuwa Wakristo wamekufuru kwa kusema kwao Mwenyezi Mungu ni mmoja wa Watatu! Tena Qur'an katika Sura hii imewasifu baadhi ya Wakristo ambao wameikubali haki na wakaiamini, na ikamkataza Muumini kujiharimishia mwenyewe vitu vizuri, na ikabainisha nini kafara ya kuvunja kiapo. Sura hii kadhaalika imeharimisha ulevi kabisa, na imebainisha ibada za Hija na cheo cha Alkaaba na miezi mitakatifu, na ikaeleza upotovu wa baadhi ya mambo waliyo jiharimishia Waarabu wenyewe kwa wenyewe bila ya hoja wala dalili yoyote, kama ilivyo bainisha wasia wakati wa safari. Mwishoe Sura hii imekhitimisha kwa kutaja miujiza iliyo tokea kwa Nabii Isa a.s. Na juu ya hiyo miujiza Banu Israili walimkanya. Pia Sura imetaja kuwa Nabii Isa a.s. hana dhambi ya walio potoka wakamuabudu, na imeeleza Ufalme wa Mwenyezi Mungu *Subhanahu* juu ya mbingu na ardhi, na ukamilifu wa uwezo wake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU, MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Enyi mlio amini! Timizeni ahadi. Mmehalalishiwa wanyama wa mifugo, ila wale mnao tajiwa. Lakini msihalalishe kuwinda nanyi mmo katika Hija. Hakika Mwenyezi

Mungu anahukumu apendavyo.¹

2. Enyi mlio amini! Msivunje hishima ya alama ya Dini ya Mwenyezi Mungu wala mwezi mtakatifu, wala wanyama wanao pelekwa Makka kuchinjwa, wala vigwe vyao, wala wanao elekea kwendea Nyumba Takatifu, wakitafuta fadhila na radhi za Mola wao Mlezi. Na mkisha toka Hija yenu basi windeni. Wala kuwachukia watu kwa kuwa wali- kuzuilieni kufika Msikiti mtakatifu kusikupelekeeni kuwafanyia uadui. Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.²

3. Mmeharimishiwa nyamafu, na damu, na nyama ya nguruwe, na mnyama aliye chinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na aliye kufa kwa kunyongeka koo, na aliye kufa kwa kupigwa, na aliye kufa kwa kuanguka, na aliye kufa kwa kupigwa pembe, aliye liwa na mnyama, ila mkimdiriki kumchinja. Na pia ni haramu kula nyama aliye chinjiwa masanamu. Na ni haramu kupiga ramli. Hayo yote ni upotovu. Leo walio kufuru wamekata tamaa na Dini yenu; basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi. Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini. Na mwenye kushurutishwa na njaa, bila ya kupendelea dhambi, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye kurehemu.³

1 Enyi Waumini! Jilazimisheni kutimiza ahadi zote baina yenu na Mwenyezi Mungu, na ahadi za kisharia zililo baina yenu na watu wengineo. Na Mwenyezi Mungu amekuhalalishieni kula nyama howa, yaani nyama wa kufuga, kama ngamia, ng'ombe, kondoo, mbuzi n.k. ila wale mlio tajiwa kuwa ni haramu. Wala haikujuzieni kuwinda barani pale mnapo kuwa mmeharimia Hija, au mpo katika eneo la ardhi takatifu. Hakika Mwenyezi Mungu huhukumu apendavyo kwa hikima yake. Yeye ndiye Muumbaji, na ndiye Mwenye kujua jema na baya la viumbe vyake. Na haya ni miongoni mwa ahadi za Mwenyezi Mungu zililo juu yenu.

2 Enyi Waumini! Msivunje hishima ya alama ya Dini ya Mwenyezi Mungu, yaani ibada alizo amrisha Mwenyezi Mungu, kama ibada za Hija wakati wa Ihram, na sharia na hukumu nyenginezo. Wala msivunje hishima ya miezi mitakatifu kwa kuzua vita katika miezi hiyo. Wala msipinge wanyama wanao pelekwa Makka, kwa kupokonya au kuzuia wasifike huko, wala msiwavue vigwe walivyo fungwa shingoni mwao kuwa ni alama kuwa wamekusudiwa kupelekwa Nyumba Takatifu, na kuwa watakuwa dhabihu wa Hija. Wala msiwapinge wanao kusudia kwenda Hija nao wakitafuta fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu. Na mkisha vua Ihram na mkatoka kwenye eneo la Alharam, basi mnaweza kuwinda mtakavyo. Wala msipelekewe na chuki yenu kubwa kwa wale walio kuzuieni kufika kwenye Msikiti wa Makka mkawafanyia uadui. Enyi Waumini! Saidianeni katika kutenda kheri na mambo yote ya ut'iifu, wala msisaidiane katika maasi, na kupindukia mipaka aliyo iweka Mwenyezi Mungu. Na ogopeni adhabu ya Mwenyezi Mungu na nguvu zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuwadhibu wale wanao mkosa. (*Tazama Maelezo 5:2*)

3 Enyi Waumini! Mwenyezi Mungu amekuharimisheni kula nyamafu, yaani aliye kufa bila ya kuchinjwa kisharia. Na damu inayo tiririka, na nyama ya nguruwe, na yule ambaye wakati wa kuchinjwa ametajiwa jina lisilo kuwa la Mwenyezi Mungu, na aliye kufa kwa kunyongwa, au aliye pigwa mpaka akafa, au aliye kufa kwa kuanguka, au kwa kupigwa pembe, au kwa kuliwa na mnyama mwingine. Ama yule mnaye mdiriki angali yu hai naye ni mnyama wa halali kuliwa, mkamchinja, basi huyo ni halali kwenu. Mwenyezi Mungu ameharimisha kula wanyama walio tolewa sadaka au mhanga kwa masanamu. Na pia ameharimisha kuagua yaliyo ghaibu kwa uganga wa kupiga ramli, na mfano wa hayo. Kula chochote katika vilivyo tajwa kuwa ni haramu ni dhambi kubwa, na ni kutoka kwenye ut'iifu wa Mwenyezi Mungu. Tangu sasa tamaa ya makafiri kuiviza Dini yenu imekwisha potea. Basi msiwaogope kuwa watakushindeni, bali ogopeni kutofuata amri zangu. Leo nimekukamiliishieni hukumu za Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu kwa kukupeni nguvu na kukuimarisheni, na nimekukhitarieni UISLAMU uwe ndiyo Dini. Lakini mwenye kulazimika kwa njaa akala kidogo katika hivyo vilivyo harimishwa, akala ili asife, bila ya kukusudia uasi, basi Mwenyezi Mungu humsamehe mtu huyo kwa kulazimika kula cha haramu asije akafa. Mwenyezi Mungu ni Mwenye huruma na rehema kwa alivyo halalisha. (*Tazama Maelezo 5:3*)

4. Wanakuuliza wamehalalishiwa nini? Sema: Mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri na mlicho wafundisha wanyama kukiwinda. Mnawafundisha alivyo kufunzeni Mwenyezi Mungu. Basi kuleni walicho kukamatieni, na mkisomee jina la Mwenyezi Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.⁴
5. Leo mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri. Na chakula cha walio pewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali kwao. Na pia wanawake wema miongoni mwa Waumini, na wanawake wema miongoni mwa walio pewa Kitabu kabla yenu, mtakapo wapa mahari yao, mkafunga nao ndoa, bila ya kufanya uhasharati wala kuwaweka kinyumba. Na anaye kataa kuamini bila shaka a'mali yake imepotea, naye katika Akhera atakuwa miongoni mwa wenye khasara.⁵
6. Enyi mlilo amini! Mnapo simama kwa ajili ya Sala basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba basi ogeni. Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni vumbi lilio safi, na mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu; bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru.⁶
7. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, na ahadi yake aliyo fungamana nanyi mlipo sema: Tumesikia na tumet'ii. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi sana wa yaliyomo vifuani.⁷
8. Enyi mlilo amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya

4 Ewe Mtume! Waumini wanakuuliza nini walicho halalishiwa katika vyakula na vyenginevyo? Waambie: Mwenyezi Mungu amekuhalalishieni kila chema kipendacho nafsi njema. Na pia amekuhalalishieni kila kinacho windwa na wanyama wenu mlilo wafunza kuwinda, kwa kutokana na alivyo kufunzeni Mwenyezi Mungu. Basi kuleni wanacho winda wanyama hao mlilo watuma, na mtaje jina la Mwenyezi Mungu pale mnapo watomeza. Na mcheni Mwenyezi Mungu kwa kuzishika sharia zake, wala msikiuke mipaka yake. Tahadharini kumkhalifu Mwenyezi Mungu katika hayo, kwani Yeye ni Mwepesi wa kuhisabu.

5 Leo, yaani tangu kuteremka Aya hii, mmehalalishiwa kila kilicho chema kipendacho nafsi njema; na pia mmehalalishiwa chakula cha Watu wa Kitabu (Mayahudi na Wakristo), na walio chinja wao, katika vitu ambavyo havikutajwa kuwa ni haramu, kama ilivyo kuwa wao ni halali kwao kula chakula chenu. Na mmehalalishiwa nyinyi kuwaoa wanawake wema wa Kiislamu na wa Ahlil Kitaab (Mayahudi na Wakristo). Hayo kwa sharti mkiwapa mahari yao kwa kusudi ya kuwaoa, sio kwa kuingiana nao kinyume na sharia kwa jahara au kwa kuwaweka mahawara kinyumba. Na mwenye kuipinga Dini, basi amepoteza malipo ya a'mali yake aliyo dhani kuwa ndiyo itamkaribisha, naye huko Akhera ni katika walio hiliki.

6 Enyi Waumini! Mkitaka kusali nanyi hamna udhu, tawadhini kwa kukosha nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake maji kichwa kizima au baadhi yake. Na mkoshe miguu yenu mpaka vifundoni. Mnapo taka kusali nanyi mna janaba kwa kuingiliana na wake zenu, basi kogeni mwili mzima. Ikiwa mna maradhi ambayo hayakufaliini kutumia maji, au mpo safarini na ipo taabu ya maji, au mmetoka chooni kukidhi haja, au mmeingiliana (kwa lugha ya Qur'ani "kugusana") na wanawake na msipate maji, basi inakupaseni kutayamamu, yaani kujipaka vumbi lilio safi. Na hayo ni kwa kupangusa kwa hilo vumbi nyuso zenu na mikono yenu. Na Mwenyezi Mungu hataki kukudhikini katika hayo anayo kuamrishi, bali anakupeni sharia za kukusafisheni ndani na nje, ili atimize neema zake juu yenu kwa uwongofu, na kubainisha na kusahilisha, mpate kumshukuru kwa uwongofu wake na kutimilia neema yake kwa kudumisha ut'iifu kwake. (*Tazama Maelezo 5:6*)

7 Kumbukeni, enyi Waumini, neema za Mwenyezi Mungu alizo kuneemesheni kwa kukuongoeni kwenye Uislamu. Jitahidini kutimiza ahadi yake aliyo itaka kwenu wakati mlipo muunga mkono Mtume wake, Muhammad, kuwa mtamsikia na mtamt'ii. Na mcheni Mwenyezi Mungu kwa kuzihifadhi ahadi hizi. Yeye, *Subhanahu*, ni Mjuzi sana wa yote yaliyo fichikana nyoyoni mwenu, naye atakulipeni kwayo.

uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.⁸

9. Mwenyezi Mungu amewaahidi walio muamini na wakatenda mema kwamba watapata maghfira na malipo makubwa.⁹

10. Na wale walio kufuru na wakakanusha Ishara zetu, hao ndio watu wa Motoni.¹⁰

11. Enyi mlio amini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, walipo taka watu kukunyooshieni mikono, naye akaizulia mikono yao kukufikieni. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.¹¹

12. Na Mwenyezi Mungu alifanya agano na Wana wa Israili. Na tukawateulia kutokana nao wakuu kumi na mbili. Na Mwenyezi Mungu akasema: Kwa yakini Mimi ni pamoja nanyi. Mkisali, na mkatoa Zaka, na mkawaamini Mitume wangu, na mkawasaidia, na mkamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, hapana shaka nitakufutieni maovu yenu na nitakuingizeni katika mabustani yapitayo mito kati yake. Lakini atakaye kufuru miongoni mwenu baada ya hayo bila ya shaka atakuwa amepotea njia iliyo sawa.¹²

13. Basi kwa sababu ya kuvunja agano lao tuliwalaani, na tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu. Wanayabadilisha maneno kutoka pahala pake, na wamesahau sehemu ya yale waliyo kumbushwa. Na huachi kuvumbua khiana kutokana nao, isipo kuwa wachache miongoni mwao. Basi wasamehe na waache. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.¹³

8 Enyi Waumini! Jitahidini kutimiza haki za Mwenyezi Mungu, na shuhudieni kwa haki baina ya watu. Chuki zenu kubwa kwa watu fulani zisikupelekeeni mkaacha kuwafanyia uadilifu. Bali jilazimisheni uadilifu, kwani hiyo ndiyo njia ya kupelekea kumcha Mwenyezi Mungu, na kuepukana na ghadhabu yake. Na mcheni Mwenyezi Mungu katika mambo yenu yote; kwani Yeye, Sub hanahu, anayajua vilivyo yote mnayo yafanya, naye atakulipeni kwayo. (Tazama Maelezo 5:8)

9 Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake amewaahidi walio isadiki Dini yake na wakatenda mema kuwa atawasamehe dhambi zao, na atawalipa badala yake thawabu.

10 Na wale wanayo ipinga Dini ya Mwenyezi Mungu, na wakakanusha Ishara zinazo onyesha Umoja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ukweli wa Ujumbe wake, hao ni watu wa kudumu katika Jahannamu.

11 Enyi Waumini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu katika wakati wa shida, pale baadhi ya Washirikina walipo kusudia kukuuweni nyinyi na Mtume wenu, Mwenyezi Mungu akazuia balaa yao isikufikieni, na akakuokoeni. Shikamaneni na kumcha Mwenyezi Mungu, na mumtegemee Yeye peke yake, katika mambo yenu. Kwani Yeye anakutosheni. Inavyo muelekea Muumini ni kumtegemea Mwenyezi Mungu peke yake daima milele.

12 Mwenyezi Mungu alichukua ahadi kutokana na Wana wa Israili kuwa watamsikia na watamt'ii. Akawateulia marais thinaashara kutokana miongoni mwao ili itimie hiyo ahadi. Na Yeye Mwenyezi Mungu akawaahidi ahadi ya nguvu kuwa atakuwa pamoja nao, atawasaidia na atawanusuru ikiwa watashika Sala kama ipasavyo, na watatoa Zaka walizo faridhiwa, na watawasadiki Mitume wake wote, na watawanusuru, na watatoa mali kwa ajili ya mambo ya kheri. Na kwamba pindi wakifanya hayo basi Mwenyezi Mungu atawafutia dhambi zao, na atawatia katika Bustani zake zipitazo mito kati yake. Na mwenye kukufuru, na akavunja ahadi baada ya hayo, basi huyo amepotoka na hakufuata njia iliyo kaa sawa iliyo nyooka.

13 Basi kwa sababu ya Wana wa Israili kuvunja agano lao ndio wakastahiki kufukuzwa kutokana na rehema ya Mwenyezi Mungu. Nyoyo zao zikawa ngumu, si laini za kupokea Haki; na wakaingia kupotoa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyomo katika Taurati kutokana na maana yake ya asli, na yafuate yanayo wafikiana na wapendavyo wao. Wakaachilia mbali pande kubwa ya mambo waliyo amrishwa katika Taurati !! Na wewe, Mtume, huachi kuona kila namna ya khadaa na uvunjaji wa ahadi kwa hawa Wana wa Israili, isipo kuwa kwa wachache tu miongoni mwao ambao wanakuamini wewe. Hao hawakhuni wala hawadanganyi. Basi, ewe Mtume! Yasamehe yaliyo pita kutokana na watu hawa, na wachilia mbali, bali wafanyie wema. Kwani Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.

14. Na kutoka kwa wale walio sema: Sisi ni Manasara, tulichukua ahadi yao, lakini wakasahau sehemu ya waliyo kumbushwa. Kwa hivyo tukaweka kati yao uadui na chuki mpaka Siku ya Kiyama. Na hapo Mwenyezi Mungu atawaambia waliyo kuwa wakiyafanya.¹⁴

15. Enyi Watu wa Kitabu! Amekwisha kujieni Mtume wetu anaye kufichulieni mengi mliyo kuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anaye samehe mengi. Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru na Kitabu kinacho bainisha.¹⁵

16. Mwenyezi Mungu huwaongoa wenye kufuata radhi yake katika njia za salama, na huwatoa katika giza kuwapeleka kwenye nuru kwa amri yake, na huwaongoa kwenye njia iliyo nyooka.¹⁶

17. Hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni Masihi mwana wa Maryamu. Sema: Ni nani mwenye kumiliki cho chote mbele ya Mwenyezi Mungu ikiwa Yeye angetaka kumuangamiza Masihi mwana wa Maryamu, na mama yake, na wote waliomo katika ardhi? Na mamlaka ya mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ni vya Mwenyezi Mungu. Huumba apendavyo. Na Mwenyezi Mungu anao uweza juu ya kila kitu.¹⁷

18. Na Mayahudi na Wakristo wanasema: Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake. Sema: Basi kwa nini anakuadhibuni kwa ajili ya dhambi zenu? Bali nyinyi ni watu tu kama wale wengine alio waumba. Humsamehe amtakaye na humuadhibu amtakaye. Na ni wa Mwenyezi Mungu tu ufalme wa mbingu na ardhi. Na marejeo ni kwake Yeye.¹⁸

19. Enyi Watu wa Kitabu! Bila ya shaka amekujilieni Mtume wetu akikubainishieni katika wakati usio kuwa na Mitume, msije mkasema: Hakufika kwetu mbashiri wala mwonyaji. Basi amekujieni mbashiri na mwonyaji. Na Mwenyezi Mungu anao uweza wa kila kitu.¹⁹

14 Hali kadhaalika Mwenyezi Mungu alichukua ahadi kwa Wakristo, ambao wamesema: Sisi ni Manasara, kwa kuwa wataiamini Injili, na watamuamini Mwenyezi Mungu Mmoja. Nao wakaacha mengi walio amrisha katika Injili. Mwenyezi Mungu akawaadhibu kwa hayo, kwa kutia uadui na khasama baina ya wao kwa wao, wakawa makundi mbali mbali yenye uadui mpaka Siku ya Kiyama. Na hapo Mwenyezi Mungu atawaambia waliyo kuwa wakiyafanya, na atawalipa kwayo.

15 Enyi Watu wa Kitabu! Amekujilieni Mtume wetu, Muhammad, akiita watu wafuate Haki. Anakufichulieni mengi mliyo kuwa mkiyaficha katika Taurati na Injili. Na anayaacha mengi katika mliyo yaficha ambayo hayana haja kuyadhihirisha. Amekuleteeni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Sharia kaamili, ambayo Sharia hiyo peke yake ni nuru, na inabainishwa na Kitabu kilicho wazi.

16 Mwenyezi Mungu kwa Kitabu hichi anawaongoa kwenye njia ya uwokofu wanao elekea kutaka radhi zake, na anawatoa kwenye giza la ukafiri kuendea mwangaza wa Imani kwa tawfiki yake, na anawaongoza kwenye njia ya Haki.

17 Hakika wamekufuru wale wanao dai ati Mwenyezi Mungu ndiye Masihi mwana wa Maryamu!! Ewe Mtume! Waambie hao wanao thubutu kuchezea cheo cha Ungu: Hapana ye yote anaye weza kuzuia matakwa ya Mwenyezi Mungu akitaka kumteketeza Isa na mama yake, na kuwahiliki wote waliomo katika ardhi. Kwani ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yao ni wa Mwenyezi Mungu peke yake. Yeye huumba mfano autakao. Na Mwenyezi Mungu ana uweza mkubwa kabisa. Hashindwi na kitu.

18 Na Mayahudi na Wakristo husema: Sisi ndio tulio fadhiliwa, kwani sisi ndio wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake atupendao. Waambie ewe Mtume! Basi kwa nini anakuadhibuni kwa dhambi zenu, na anakutieni katika moto wa Jahannamu? Waongo nyinyi! Nyinyi, kama wanaadamu wengineo, ni viumbe, na mtahisabiwa kwa vitendo vyenu. Na maghfira yamo mikononi mwa Mwenyezi Mungu peke yake, humsamehe amtakaye. Na adhabu yake ni kwa amtakaye kumuadhibu. Kwani ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yao ni wa Mwenyezi Mungu tu, na kwake Yeye ndio marejeo ya mwisho.

19 Enyi Watu wa Kitabu! Umekujieni ujumbe wa Mtume wetu ambaye anakudhihirishieni Haki, baada ya

20. Na pale Musa alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, alipo wateuwa Manabii kati yenu, na akakufanyeni watawala, na akakupeni ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu.²⁰
21. Enyi watu wangu! Ingieni katika nchi takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amekuandikieni. Wala msirudi nyuma, msije mkawa wenye kukhasirika.²¹
22. Wakasema: Ewe Musa! Huko wako watu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka wao watoke humo. Wakitoka humo hapo tutaingia.²²
23. Watu wawili miongoni mwa wachamngu ambao Mwenyezi Mungu amewanemesha, walisema: Waingilieni kwa mlangoni. Mtakapo waingilia basi kwa yakini nyinyi mtashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini.²³
24. Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa.²⁴
25. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu. Basi tutenge na hawa watu wapotovu.²⁵
26. (Mwenyezi Mungu) akasema: Basi nchi hiyo wameharimishiwa muda wa miaka arubaini, watakuwa wakitanga-tanga katika ardhi. Basi wewe usiwasikitikie watu wapotovu.²⁶
27. Na wasomee khabari za wana wawili wa Adam kwa kweli. Walipo toa mhanga, ukakubaliwa wa mmoja wao, na wa mwengine haukukubaliwa. Akasema: Nitakuuwa. Akasema mwengine: Mwenyezi Mungu huwapokelea wachamngu.²⁷

kusita ujumbe kwa muda wa zama, ili msitafute udhuru wa ukafiri wenu, kwa kudai ati kuwa Mwenyezi Mungu hakukuleteni mbashiri wa kukupeni khabari njema, wala mwonyaji wa kukuhadharisheni. Sasa, basi, huyo amekujilieni mbashiri na mwonyaji. Na Mwenyezi Mungu ni muweza wa kila jambo - na katika hayo mambo ni kutuma Mitume, na kukuhisabuni kwa mliyo nayo.

20 Na taja, ewe Mtume! pale Musa alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu kwa kushukuru na kut'ii, kwa kuwa amewateua Manabii wengi miongoni mwenu, na akakufanyeni watukufu kama wafalme baada ya kuwa mlikuwa wanyonge chini ya utawala wa Firauni, na akakupeni neema nyingi nyenginezo ambazo hawajapewa wowote wengineo.

21 Enyi watu wangu! T'iiini amri ya Mwenyezi Mungu. Ingieni ardhi takatifu aliyi kujaalieni Mwenyezi Mungu muingie, wala msirejee nyuma kuwaogopa hao watu wake majabari, mkaja kukosa nusura ya Mwenyezi Mungu na radhi zake.

22 Wana wa Israili wakaikhalifu amri ya Mwenyezi Mungu na wakasema: Ewe Musa! Katika nchi hii wamo watu majabari. Sisi hatuna nguvu za kupambana nao. Basi hatutoingia humo maadamu wao wamo. Wakitoka basi tena hapo sisi tutaingia.

23 Wawili kati ya wakubwa wao walio kuwa wanamwogopa Mwenyezi Mungu, na ambao Mwenyezi Mungu amewapa neema ya imani na ut'iifu, walisema: Enyi watu! Waingilieni hao majabari wa mjini kwa kupitia mlangoni kwa ghafla. Mkifanya hivyo nyinyi mtawashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu peke yake katika mambo yenu yote, ikiwa nyinyi ni wenye Imani ya kweli.

24 Lakini wakakakamia katika ukhalifu wao. Wakasema: Ewe Musa! Sisi bila ya shaka yoyote tumekwisha azimia kuwa hatutaingia nchi hii kabisa, maadamu wamo hao majabari. Basi tuache na yetu; kwani wewe huna madaraka yoyote juu yetu. Nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane nao hao majabari. Sisi tutakaa hapa hapa hatubanduki.

25 Hapo tena Musa akamreja Mola wake Mlezi akisema: Mola wangu Mlezi! Sina madaraka ila juu ya nafsi yangu na ndugu yangu. Basi tuhukumie baina yetu na hawa watu wakaidi.

26 Mwenyezi Mungu akamuitikia Musa, akawapigia marfuku hao wakhalifu wasiingie nchi hiyo kwa muda wa miaka arubaini, wakipotewa ovyo majangwani hawajui wendako wala watokako. Mwenyezi Mungu akamwambia Musa kama kumuasa: Usisikitike kwa masaiibu yaliyo wasibu, kwani hawa ni wapotovu, wameiasi amri ya Mwenyezi Mungu.

27 Hakika kupenda kutenda uadui ni tabia ya baadhi ya watu. Basi ewe Nabii! Wasomee Mayahudi - na wewe ni msema kweli - khabari za Haabila na Qaabila, wana wawili wa Adam. Kila mmoja alichinja

- 28.** Ukininyooshea mkono wako kuniuwa, mimi sitakunyoooshea mkono wangu kukuuwa. Hakika mimi namwogopa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.²⁸
- 29.** Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako, kwani wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni. Na hayo ndiyo malipo ya wenye kudhulumu.²⁹
- 30.** Basi nafsi yake ikampelekea kumuwa nduguye, akamuwa na akawa miongoni mwa wenye kukhasirika.³⁰
- 31.** Hapo Mwenyezi Mungu akamleta kunguru anaye fukua katika ardhi ili amwonyeshe vipi kumsitiri nduguye. Akasema: Ole wangu! Nimeshindwa kuwa kama kunguru huyu nikamsitiri ndugu yangu? Basi akawa miongoni mwa wenye kujuta.³¹
- 32.** Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote. Na hakika waliwajia Mitume wetu na hoja zilizo wazi. Kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi.³²
- 33.** Basi malipo ya wale wanao mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawania kufanya uchafuzi katika nchi, ni kuuwawa, au kusalibiwa, au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kutolewa nchi. Hii ndiyo hizaya yao katika dunia; na katika Akhera watapata adhabu kubwa.³³

dhabihu kama ni mhanga kwa kutaka kuruba kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu alimkubalia mmoja kwa ajili ya usafi wa niya yake, na akamkatalia wa pili kwa kuwa niya yake haikuwa safi. Basi yule aliye kataliwa akamhusudu mwenzie na akamuahidi kuwa atamuwa. Yule nduguye akamrudi kwa kumbainishia kuwa Mwenyezi Mungu hapokei a'mali ila kwa wachamngu walio safisha niya zao katika kule kutafuta kuruba.

28 Akamwambia: Shetani akikuzuga hata ukaninyooshea mkono ili kuniuwa, mimi sitofanya kama hivyo, wala sitanyoosha mkono wangu kwa ajili ya kukuuwa. Hakika mimi naogopa adhabu ya Mola wangu Mlezi, naye ndiye Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.

29 Mimi sitakuzuia utapo taka kuniuwa ili upate kubeba dhambi za kuniuwa mimi pamoja na dhambi zako za tangu hapo za kutomsafia niya Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo wewe unastahiki huko Akhera kuwa katika watu wa Motoni. Na hayo ni malipo ya haki ya Mwenyezi Mungu kumlipa kila mwenye kudhulumu.

30 Basi nafsi yake ilimsahilishia kukhalifiana na maumbile, kumuwa nduguye, akamuwa. Kwa hivyo akawa kwa mujibu wa hukumu ya Mwenyezi Mungu miongoni mwa walio khasiri, kwa kuwa ameipoteza imani yake na amempoteza nduguye.

31 Baada ya kumuwa yakamjia majuto na kubabaika. Akawa hajui amfanyeje maiti! Mwenyezi Mungu akampeleka kunguru akafukua udongo amzike kunguru mwengine aliye kufa, ili amfunze muuwaji vipi kumsitiri mwenzake aliye kwisha kufa. Alipo hisi uovu wa aliyo yatenda, alijuta kwa ukhalifu wake, akasema: Nimeshindwa hata kuwa kama kunguru huyu nikamsitiri ndugu yangu? Akawa basi miongoni wa walio juta kwa makosa yake, na kwenda kinyume na yanavyo takikana na maumbile.

32 Kwa sababu ya uasi huo na kupenda kwa baadhi ya watu kuwafanyia uadui wengine, ndio tukawajibisha kumuwa muuwaji, kwani mwenye kumuwa mtu bila ya sababu zinazo pasa kisasi, au bila ya kufanya uharibifu katika nchi, ni kama amewauwa watu wote. Yeye huyo amemwaga damu za watu, na amewashajiisha wengine wafanye kama hayo. Kwa hivyo kumuwa mmoja ni kama kuwauwa watu wote kwa kujiletea maudhiko ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake. Na mwenye kumhuisha mtu kwa kumlipia kisasi, basi ni kama amewahuisha watu wote kwa kuhifadhi damu ya wanaadamu isimwagwe ovyo. Huyu anastahiki thawabu nyingi kutokana na Mola wake Mlezi. Sisi tumewatumia Mitume wetu kutilia mkazo hukumu yetu kwa dalili na hoja. Kisha baadaye wengi miongoni mwa Wana wa Israili walipindukia mipaka katika uharibifu wao katika nchi. (*Tazama Maelezo 5:32*)

33 Hakika adhabu ya wale wanao mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kuacha hukumu za Sharia, na wakafanya uharibifu katika nchi kwa uharamia na kunyan'ganya mali, ni kuuliwa pindi wakiuwa, na kutundikwa msalabani, pindi wakiuwa na wakapokonya mali ya watu, na kukatwa mikono

- 34.** Isipo kuwa wale walio tubu kabla hamjawatia nguvuni. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu.³⁴
- 35.** Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na tafuteni njia ya kumfikilia. Na wanieni kwa juhudi kwa ajili yake ili mpate kuokoka.³⁵
- 36.** Hakika walio kufuru lau wange kuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya Siku ya Kiyama, yasingeli pokelewa kwao; na watapata adhabu chungu.³⁶
- 37.** Watataka watoke Motoni, lakini hawatatoka humo, na watakuwa na adhabu inayo dumu.³⁷
- 38.** Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao, hayo ni malipo ya waliyo yachuma, ndiyo adhabu ya mfano itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.³⁸
- 39.** Lakini mwenye kutubia baada ya dhulma yake, na akatengenea, basi Mwenyezi Mungu atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu.³⁹
- 40.** Hujui ya kwamba Mwenyezi Mungu anao ufalme wa mbingu na ardhi? Humuadhibu

yao na miguu kwa mabadilisho (yaani mkono wa kulia na mguu wa kushoto, au kinyume cha hayo), pindi ikiwa watavamia watu njiani na kuwapokonya mali bila ya kuwauwa. Na ikiwa watawatisha watu tu, basi adabu yao ni kuhamishwa nchi au wafungwe. Adhabu hizo ni hizaya ya hapa duniani tu, na Akhera watapata adhabu kuu, nayo ni adhabu ya Motoni.

34 Ila wale walio tubu, miongoni mwa hawa wanao piga vita nidhamu na wakavamia watu majiani, kabla hamjawatia mkononi mkawakamata. Basi adhabu ya Mwenyezi Mungu itaondoka, itabaki juu yao haki za waja wa Mwenyezi Mungu wazirejeshe. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira na rehemu. (*Tazama Maelezo 5:34*)

35 Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu kwa kujitenga na anayo yakataza, na kut'ii amri zake. Na takeni kuyafanya yatakayo kukurubisheni kupata thawabu zake, nayo ni kutenda mambo ya ut'ifu na mambo ya kheri. Na wanieni kwa jihadi katika Njia yake kwa kuitukiza Dini yake na kuwapiga vita maadui zake. Huenda kwa hivyo mkafuzu mkapata karama zake na thawabu zake.

36 Hakika walio kufuru hata lau kuwa wana kila namna ya mali yote yaliyomo duniani na mambo mengine yanayo onekana yenye maana katika uhai, na wakawa nayo mfano wa yaliyomo duniani juu ya hayo yaliyomo humo, na wakataka yawe ni fidiya wajiokoe na adhabu ya Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama kwa ukafiri wao, basi fidiya hiyo yote haitofaa kitu. Wala Mwenyezi Mungu hawakubalii hayo. Hapana njia yo yote ya wao kuepukana na malipo ya ukafiri wao; nao watapata adhabu kali.

37 Hawa makafiri wanatamani kutoka Motoni, na wala hawatatoka humo. Watapata adhabu ya daima dawamu.

38 Na mwanamume aliye iba, na mwanamke aliye iba, ikateni mikono yao kuwa ni malipo ya madhambi waliyo yatenda, na njia ya kuwaonya wenginewe wasitende jambo hilo. Hiyo ni hukumu ya Mwenyezi Mungu, na amri ya Mwenyezi Mungu ndiyo yenye kushinda, naye ndiye Mwenye hikima katika kutunga Sharia. Kila ukhalifu ameuwekea malipo yake, yenye kumzuia mtu asitende tena na wengine watahadhari wasifanye kama hayo. (Ajabu iliopo ni kuwepo wajinga wakashitushwa na amri hii ya Mwenyezi Mungu aliye tuumba, na wasiseme lolote kuwa katika China wakati wa vita na Taiwan ilikuwapo sharia ya kuwa mwizi auwawe, na katika baadhi ya wilaya za Amerika mpaka hii leo ipo sharia ya kuwa mwizi wa farasi auwawe, na katika Kenya adabu ya wizi wa kutumia nguvu ni kunyongwa, na katika sharia za Kiingereza na nchi zote za magharibi mtu ana haki ya kuuwa kwa ajili ya kulinda mali na roho. Ikiwa ni haki ya mtu kumuwa atakaye kuja kwiba, jee ni kuu hilo kwa serikali kumkata mkono aliye kwisha iba?) Kwa kuwepo sharia kama hii ndiyo ikawa wizi umetoweka katika nchi kama Saudi Arabia, na ukawa vururu kwengineko.

39 Lakini mwenye kutubu baada ya kutenda kosa lake hilo, na akatengeneza vitendo vyake, na akanyoosha mwendo wake, basi Mwenyezi Mungu hakika humkubalia toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwingi mno wa kusamehe na kurehemu.

amtakaye, na humsamehe amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.⁴⁰

41. Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wa fanyao haraka kukufuru, miongoni mwa wanao sema kwa vinywa vyao: Tumeamini, na hali nyoyo zao hazikuamini, na miongoni mwa Mayahudi, wanao sikiliza kwa ajili ya uwongo, wanao sikiliza kwa ajili ya watu wengine wasio kufikia. Wao huyabadilisha maneno kutoka pahala pake. Wanasema: Mkipewa haya basi yashikeni, na msipo pewa haya tahadharini. Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumfitini huwezi kuwa na madaraka naye mbele ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo zao. Watakuwa na hizaya duniani, na Akhera watakuwa na adhabu kubwa.⁴¹

42. Hao ni wasikilizaji kwa ajili ya kusema uwongo, na ni walaji mno vya haramu! Basi wakikujia, wahukumu baina yao au jipuuze nao. Na ukijipuuza nao, basi wao hawatakudhuru kitu. Na ukiwahukumu, basi hukumu baina yao kwa uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda waadilifu.⁴²

43. Na huwaje wakufanye wewe hakimu nao wanayo Taurati yenye hukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanageuka. Na hao si wenye kuamini.⁴³

44. Hakika Sisi tuliteremsha Taurati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii walio nyenyekea kiislamu, na wachamngu, na wanazuoni, waliwahukumu Mayahudi; kwani walikabidhiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Nao wakawa ni mashahidi juu yake. Basi msiwaogope watu, bali niogopeni Mimi. Wala msibadilishe Aya zangu kwa thamani chache. Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.⁴⁴

40 Jua, ewe mwenye fahamu, kwa ujuzi wa yakini, ya kwamba ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kumiliki kila kitu kiliomo katika mbingu na ardhi. Yeye humpa adhabu yake amtakaye, kwa hikima yake na uwezo wake. Na humsamehe amtakaye, kwa hikima yake na rehema yake. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

41 Ewe Mtume! Visikuhuzunishe vitendo vya makafiri wanao wania ukafiri wa kila aina, hawa wadanganyifu wenye khadaa wasemao kwa ndimi zao: Tumeamini, ilhali nyoyo zao hazifuati haki. Na miongoni mwa Mayahudi wapo wanao kithiri kusikiliza uzushi wa makohani wao na wanayakubali, na wanakisikiliza na kukikubali kikundi maalumu miongoni mwao, na hawaji barazani kwako kwa sababu ya kiburi na chuki! Na hawa huyageuza maneno ya Taurati kutokana pahala pake, baada ya Mwenyezi Mungu kwisha yasimamisha na kuyahukumu! Nao huwaambia wafwasi wao: Mkipewa maneno haya yaliyo potoshwa na kubadilishwa yakubalini na muyafuate. Na kama mkipewa mengine tahadharini nayo msiyakubali. Basi, ewe Mtume! Usihuzunike Mwenyezi Mungu akimhukumu mtu kupotea kwa kumziba moyo wake, wewe hutoweza kumwongoa, au kumnafiisha kwa chochote asicho mtakia Mwenyezi Mungu. Na hao ndio walio pita mipaka katika upotovu na inda. Mwenyezi Mungu Mwenyewe hakutaka kuzisafisha nyoyo zao na uchafu wa chuki, na inadi, na ukafiri. Duniani watapata madhila, kwa kufedheheka na kushindwa, na Akhera watapata adhabu kuu.

42 Hao hukithiri kusikiliza ili wapate kuzua, na hukithiri kula mali ya haramu ambayo hayana baraka yoyote, kama vile rushwa na riba na mengineyo. Basi wakikujia kukutaka uwahukumu, wewe wahukumu pindi ukiona hayo yana maslaha, au jipuuze nao. Na ukijipuuza nao hawatokudhuru kwa lolote, kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye wa kukulinda na watu. Na ukihukumu baina yao basi hukumu kwa uadilifu alio kuamrisha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda waadilifu, naye huwahifadhi na huwalipa thawabu.

43 Ama ajabu ya watu hawa Mayahudi! Vipi wanataka hukumu yako na hali wao wanayo hukumu ya Mwenyezi Mungu imeandikwa katika Taurati? Na kinacho staajibisha ni kuwa wao huikataa hukumu yako inapo kuwa haikubaliani na mapendeleo yao, ijapo kuwa imewafikiana na ilivyo katika kitabu chao! Watu hawa sio miongoni mwa Waumini wanaoit'ii Haki..

44 Hakika Sisi tumemteremshia Musa Taurati. Ndani yake mna uwongofu unao endea Haki, na mna bayana yenye kutoa mwangaza unao nawirisha hukumu wanazo zihukumia Manabii, na wale walio safisha

45. Na humo tuliwaandikia ya kwamba roho kwa roho, na jicho kwa jicho, na pua kwa pua, na sikio kwa sikio, na jino kwa jino, na kwa majaraha kisasi. Lakini atakaye samehe basi itakuwa ni kafara kwake. Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu.⁴⁵

46. Na tukawafuatishia hao Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Taurati, na tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongofu, na nuru na inayo sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Taurati, na uwongofu na mawaidha kwa wachamngu.⁴⁶

47. Na wahukumu Watu wa Injili kwa yale aliyo teremsha Mwenyezi Mungu ndani yake. Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu.⁴⁷

48. Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda. Basi hukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamano yao ukaacha Haki iliyo kujia. Kila mmoja katika nyinyi tumemwekea sharia yake na njia yake. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka ange kufanyeni nyote umma mmoja, lakini ni kukujaribuni kwa aliyo kupeni. Basi shindaneni kwa mambo ya kheri. Kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo yenu nyote, na atakuja kuwaambieni yale mliyo kuwa mkikhitalifiana.⁴⁸

nafsi zao kwa ajili ya Mola wao Mlezi, na wanazuoni wenye kufwata njia ya Manabii, na wale walio chukua ahadi kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu kisibadilishwe, kwa kukilinda na kushuhudia kuwa hicho ndiyo Haki. Basi msiwakhofu watu mnapo hukumu, na nikhofuni Mimi tu, Mimi Mola wenu Mlezi, Mola Mlezi wa walimwengu wote. Wala msizibadilisha Aya zangu nilizo ziteremsha kwa thamani duni ya kutaka starehe ya dunia, kama vile mrungura au kutaka cheo! Na wote wasio hukumu kwa mujibu alivyo teremsha Mwenyezi Mungu ni miongoni mwa makafiri.

45 Tumewalizimisha Mayahudi katika Taurati wafuate sharia ya kisasi kwa ajili ya kuhifadhi maisha ya watu. Basi tukahukumu mwenye kuuwa auwawe. Mwenye kutofoa jicho la mtu atofolewe. Kadhaalika pua kwa pua, sikio kwa sikio, jino kwa jino, na jaraha hivyo hivyo lilipiziwe kisasi ikimkinika. (Hiyo ni hukumu ya Mayahudi kama ilivyo katika Kutoka 21.23-25; Mambo ya Walawi 24.18-21; Kumbukumbu la Torati 19.21. Katika Uislamu ipo fursa ya msamaha.)

Mwenye kusamehe akatolea sadaka ile haki ya kulipiza kisasi kwa mkhalifu, basi hiyo sadaka huwa ni kafara kwake. Mwenyezi Mungu naye atamfutia sehemu ya madhambi yake. Na watu wasio hukumu kwa mujibu wa alivyo teremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wenye kudhulumu.

46 Na baada ya hawa Manabii tulimtuma Isa mwana wa Maryamu, naye ni mwenye kufuata njia yao, na kuithibitisha Taurati iliyo mtangulia. Naye tulimteremshia Injili yenye uwongofu kuelekea Haki, na yenye kubainisha hukumu, na tuliiteremsha ili isadikishe Taurati iliyo tangulia, na ndani yake pana uwongofu wa kupelekea Haki, na ni mawaidha kwa wachamngu. (Tazama Injili ya Mathayo 5.17 maneno ya Nabii Isa: "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza.")

47 Na Sisi tuliwaamrisha wafuasi wa Isa, yaani Watu wa Injili, Wakristo, wahukumu kwa hukumu alizo teremsha Mwenyezi Mungu. Na wasio hukumu kwa mujibu wa alivyo teremsha Mwenyezi Mungu basi hao wameiacha Sharia ya Mwenyezi Mungu, ni waasi.

48 Na wewe, ewe Nabii, tumekuteremshia Kitabu kikamilifu, nacho ni Qur'ani, chenye kushikamana na haki katika hukumu zake zote na khabari zake, chenye kuwafikiana na kuthibitisha Vitabu vyetu vilivyo tangulia, na kinavishuhudia kuwa ni Vitabu vya Mwenyezi Mungu, na kinalinda yaliyo sahihi, kwa sababu hii Qur'ani haibadiliki. Basi hukumu baina ya Watu wa Kitabu, Mayahudi na Wakristo, wakikutaka uwahukumu kwa mujibu alivyo kuteremshia Mwenyezi Mungu. Wala katika hukumu yako usifuate matamano yao na matakwa yao, usije ukapotoka ukaacha Haki iliyo kujia. Kila umma katika nyinyi watu, tumeujaalia kuwa na njia yake ya kuitambua Haki, na njia iliyo wazi ya Dini ya kuifuata. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka angeli kufanyeni nyote kundi moja lililo wafikiana, lenye mwendo mmoja, hazikhitalifiani njia zake za kupita kwa zama zote. Lakini Yeye amekujaalieni hivi ili iwe kama mthani kwenu katika hizo Sharia alizo kupeni, atambulikane mwenye kut'ii na mwenye

49. Na wahukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuata matamano yao. Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaacha baadhi ya aliyo kuteremshia Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka, basi jua kwamba hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao. Na hakika wengi wa watu ni wapotofu.⁴⁹

50. Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?⁵⁰

51. Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu.⁵¹

52. Utawaona wale wenye maradhi nyoyoni mwao wanakimbilia kwao wakisema: Tunakhofu yasisibu mabadiliko. Huenda Mwenyezi Mungu akaleta ushindi au jambo jingine litokalo kwake wakawa wenye kujuta kwa waliyo yaficha katika nafsi zao.⁵²

53. Na walio amini watasema: Hivyo hawa ndio wale walio apa ukomo wa viapo vyao kuwa wao wa pamoja nanyi? Vitendo vyao vitapotea bure, na wataamkia kuwa wenye kukhasirika.⁵³

54. Enyi mlio amini! Atakaye iacha miongoni mwenu Dini yake, basi Mwenyezi Mungu atakuja leta watu anao wapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa Waumini na wenye nguvu juu ya makafiri, wanapigania Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anaye laumu. Hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu,

kuasi. Basi tumieni fursa hii, na mfanye haraka kuwania kutenda vitendo vya kheri. Kwani marejeo yenu nyote yatakuwa kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Hapo atakwambieni hakika ya hayo mliyo kuwa mkikhitalifiana, na kila mmoja wenu atalipwa kwa a'mali yake.

49 Na wewe ewe Mtume! Tumekuamrisha uhukumu baina ya watu kwa alivyo teremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuata matakwa yao katika kuhukumu. Na wahadharishe wasije kugeuka ukaacha baadhi ya aliyo kuteremshia Mwenyezi Mungu. Pindi wakiipuuza hukumu ya Mwenyezi Mungu na wakataka nyengineyo, basi jua kuwa Mwenyezi Mungu anataka kuwapatiliza kwa kuwafisidia mambo yao, kwa vile zilivyo kwisha fisidika nafsi zao kwa sababu ya madhambi yao waliyo yatenda kwa kukhalifu hukumu zake na Sharia yake. Kisha atawalipa vitendo vyao vyote huko Akhera. Na hakika watu wengi ni wenye kuziasi hukumu za Sharia. (Tazama Maelezo 5:49)

50 Je, hao wanao kataa amri na makatazo ya Mwenyezi Mungu wanataka wahukumiwe kwa hukumu ya Kijahiliya, ya kijinga, ya kabla ya kufika Uislamu, kulipo kuwa hapana uadilifu, bali matamano ya nafsi tu ndiyo yliyo kuwa yakihukumu, na mapendeleo na udanganyifu ndio msingi wa hukumu? Huo ndio mwendo wa watu wa zama za Kijahiliya! Yuko aliye bora kuliko Mwenyezi Mungu kuhukumu watu wenye kuyakinika na Sharia na wenye kunyenyekea Haki? Kwa hakika hao ndio wanao tambua ubora wa hukumu za Mwenyezi Mungu.

51 Enyi mlio amini! Si halali kwenu kuwachukua Mayahudi na Wakristo mkawafanya ndio marafiki zenu. Wao hao ni sawa sawa katika kukufanyieni uadui. Na mwenye kufanya urafiki nao, basi ni kundi moja nao. Na hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi wanao jidhulumu nafsi zao kwa kufanya urafiki na makafiri.

52 Ilivyo kuwa kuwafanya hao marafiki hawafanyi ila walio dhulumu, basi utaona kuwa wanao wafanya makafiri ndio rafiki zao wana maradhi katika nyoyo zao, maradhi ya udhoofu na unaafiki. Wao husema: Tunaogopa usije kutupata msiba kwa kugeuka mambo na wao wasitusaidie! A'saa, huenda, Mwenyezi Mungu akamletea Mtume wake kufunguka mambo, na Waislamu wakawashinda maadui zao, au ukadhirihi unaafiki wa hao wanaafiki, wakaamkia majuto, wakijuta kwa zile kufuru na shaka shaka walizo kuwa wakizificha katika nafsi zao.

53 Na hapo tena Waumini wa kweli watasema kuwastaajabia wanaafiki: Ndio hawa walio kula yamini kwa viapo vya kupita kiasi kwa jina la Mwenyezi Mungu, ya kwamba wao ni wenzenu katika Dini, wenye kuamini kama nyinyi? Wamesema uwongo! Na vitendo vyao vimefisidika, wakawa wamekosa Imani na nusura kutokana na Waumini.

humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu na Mwenye kujua.⁵⁴

55. Hakika rafiki yenu mlinzi ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walio amini, ambao hushika Sala na hutoa Zaka nao wananyenyekea.⁵⁵

56. Na atakaye fanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walio amini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda.⁵⁶

57. Enyi mlio amini! Msiwafanye marafiki wale walio ifanyia kejeli na mchezo Dini yenu miongoni mwa walio pewa Kitabu kabla yenu, na makafiri wengine. Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini.⁵⁷

58. Na mnapo adhinia Sala wao wanaichukulia maskhara na mchezo. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.⁵⁸

59. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Hivyo mnatuchukia kwa kuwa tumemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyo teremshiwa na yaliyo teremshwa kabla, na kwa kuwa wengi katika nyinyi ni wapotofu?⁵⁹

60. Sema: Je! Nikwambieni yule ambaye ni mwenye malipo mabaya zaidi kuliko hayo mbele ya Mwenyezi Mungu? Ni yule ambaye Mwenyezi Mungu amemlaani na amemkasirikia, na amewafanya miongoni mwao manyani na nguruwe, na wakamuabudu Shet'ani. Hao ndio wenye mahali pabaya na wamepotea zaidi njia iliyo sawa.⁶⁰

61. Na wanapo kujieni husema: Tumeamini. Lakini hakika wao wameingia na ukafiri wao, na wametoka nao pia. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi kabisa wa yote wanayo yaficha.⁶¹

54 Enyi mlio amini! Mwenye kurejea ukafrini katika nyinyi, baada ya kuamini, hamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Yeye ametukuka na hayo. Badala yao ataleta kaumu iliyo bora kuliko hao, na wao hao Mwenyezi Mungu atawapenda, na atawafikisha kwenye uwongofu, na ut'iifu. Na wao watampenda Mwenyezi Mungu, kwa hivyo watamt'ii. Nao watakuwa na unyenyekevu na huruma kwa ndugu zao Waumini, na watakuwa wakali na wenye nguvu mbele ya maadui zao makafiri. Watapigana jihadi kwa njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama yoyote ya mwenye kulaumu! Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye anaye muwafikia kheri. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa fadhila kwa anaye stahiki.

55 Enyi Waumini! Urafiki wenu nyinyi uwe na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na nyinyi kwa nyinyi katika wanao shika Sala, na wanatoa Zaka, nao wananyenyekea.

56 Na mwenye kufanya urafiki na Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Waumini na wakawa hao ndio wa kuwategemea kwa msaada na nusura, basi huyo atakuwa katika Hizbu (yaani kundi) ya Mwenyezi Mungu, na Hizbu ya Mwenyezi Mungu ndio yenye kushinda na kufuzu.

57 Enyi mlio amini! Msiwafanye maadui wa Uislamu walio ifanyia maskhara Dini yenu wakaichezea - nao ni Mayahudi na Wakristo na washirikina, kuwa ndio wasaidizi, wala msifanye urafiki nao. Na mkhofuni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni wakweli katika Imani yenu.

58 Na katika kejeli zao kukufanyieni ni vile pale mnapo ita kwenda kusali katika adhana, wao huifanyia maskhara Sala yenu, na hukuchekeni, wakafanya ni mchezo. Na hayo ni kwa sababu kuwa wao ni kaumu wasio na akili, wala hawatambui farka iliopo baina ya upotofu na uwongofu.

59 Sema ewe Mtume! Enyi Watu wa Kitbu! Hivyo mnatuchukia kwa kuwa tunamuamini Mwenyezi Mungu na tunaamini tuliyo teremshiwa sisi, nayo ni Qur'ani, na Vitabu vilio sahihi vilio teremshiwa Manabii wa zamani, na kwa kuwa tunaamini kuwa wengi wenu mmeitupa Sharia ya Mwenyezi Mungu?

60 Waambie: Nikwambieni malipo maovu kabisa kutokana na Mwenyezi Mungu? Ni hivyo vitendo vyenu nyinyi mlio tengwa mbali na Mwenyezi Mungu na rehema yake, na mkakasirikiwa kwa sababu ya ukafiri wenu na uasi wenu, na mkazibwa nyoyo zenu, mkawa kama manyani na nguruwe, na mkamuabudu Shetani, na mkafuata upotovu. Nyinyi ndio mko katika daraja ya mwisho katika shari, kwa sababu nyinyi ni watu walio potea kabisa, mkaiwacha Njia ya Haki.

61 Wanaafiki wakikujia husema uwongo, na hukwambia: Tumeamini. Nao wamekuingilia na hali ni makafiri, na wametoka kwenu nao ni makafiri vile vile! Na Mwenyezi Mungu anaujua vyema unaafiki

- 62.** Na utawaona wengi katika wao wanakimbilia kwenye dhambi, na uadui, na ulaji wao vya haramu. Ni maovu mno hayo wayatendayo!⁶²
- 63.** Mbona hao wanazuoni na makohani wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi, na ulaji wao vya haramu? Ni maovu mno hayo wayafanyayo!⁶³
- 64.** Na Mayahudi walisema: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba. Mikono yao ndiyo iliyo fumba, na wamelaaniwa kwa sababu ya waliyo yasema. Bali mikono yake iwazi. Hutoa apendavyo. Kwa yakini yaliyo teremshwa kwako kutoka kwa Mola wako Mlezi yatawazidisha wengi katika wao uasi na kufuru. Na Sisi tumewatilia uadui na chuki baina yao mpaka Siku ya Kiyama. Kila mara wanapo washa moto wa vita, Mwenyezi Mungu anauzima. Na wanajitahidi kuleta uharibifu katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu hawapendi waharibifu.⁶⁴
- 65.** Na lau kuwa Watu wa Kitabu wangeli amini na wakachamngu hapana shaka tungeli wafutia makosa yao, na tungeli waingiza katika Bustani zenye neema.⁶⁵
- 66.** Na lau kuwa wangeli ishika Taurati na Injili na yote waliyo teremshiwa kutokana na Mola wao Mlezi, basi hapana shaka wangeli kula vya juu yao na vya chini ya miguu yao. Wapo watu miongoni mwao walio sawa, lakini wengi wao wanayo yafanya ni mabaya mno.⁶⁶
- 67.** Ewe Mtume! Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri.⁶⁷
- 68.** Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Hamna lenu jambo mpaka muishike Taurati na Injili

wanao uficha. Na Yeye ndiye atakaye waadhibu.

62 Na utawaona wengi wao hawa wanakimbilia kufanya maasi na kuwatendea uadui wengineo, na pia katika kula mali ya haramu kama rushwa (mrungura) na riba! Uwovu gani huu wautendao.

63 Si ingelikuwa vyema lau kuwa wanazuoni wao na makohani wangeli wakataza kusema uwongo, na kula haramu? Uwovu mkubwa huo wanao ufanya kwa kuacha kusemezana na kukatazana maasi.

64 Mayahudi walisema: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba, haukukunjuka ukatoa! Mwenyezi Mungu amefumba mikono yao wao, na amewatenga mbali na rehema yake! Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, anajitoshia. Yeye hutoa apendavyo. Na hakika wengi wa watu kwa kupita kiasi katika upotovu wao, haya yalio teremka kwako huwazidisha udhalimu na ukafiri, kwa sababu ya chuki na husda yao. Na Sisi tumetia baina yao kwa wao uadui na bughdha mpaka Siku ya Kiyama. Kila wanapo washa moto kumpiga vita Mtume na Waumini, Mwenyezi Mungu huuzima kwa kumpa ushindi Nabii wake na wafuasi wake. Na wao wanajitahidi kueneza fisadi katika nchi, na kufanya vitimbi, na kutia fitina, na kuchochea vita. Na Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi.

65 Na lau kuwa Watu wa Kitabu, yaani Mayahudi na Wakristo, wangeli uamini Uislamu na Nabii wake, na wakaacha madhambi tuliyo yataja, tungeli wafutia makosa yao, na tungeli watia katika Bustani (Pepo) za neema, wakastarehe humo.

66 Na lau kuwa wao wamezihifadhi Taurati na Injili kama zilivyo teremshwa, na wakazitenda, na wakaamini yote waliyo teremshiwa kutokana na Mola wao Mlezi, nayo ni Qur'ani, Mwenyezi Mungu angeli wakunjulia riziki ikiwajia kutoka kila upande. Na wao si wote sawa katika upotovu. Miongoni mwao, wapo jamaa walio waadilifu, wana akili zao timamu. Hao ndio wale walio muamini Muhammad na wakaamini Qur'ani. Lakini wengi wao wanatenda vitendo viovu, na wanasema mabaya, na wanajitenga na haki.

67 Ewe uliye tumwa na Mwenyezi Mungu! Waeleze watu yote uliyo funuliwa na Mola wako Mlezi, na waite wafuate huo ujumbe, wala usiogope maudhi ya yeyote. Na ukitofanya hivyo basi imekuwa hukufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Kwani wewe umekalifishwa ufikishe ujumbe kwa watu wote. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na maudhi ya makafiri. Ni mtindo wake Mwenyezi Mungu kuwa hamnusuru aliye potea akaiacha Haki. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi makafiri kwenye Njia iliyo kaa sawa.

na yote mlio teremshiwa kutokana na Mola wenu Mlezi. Na hakika ulio teremshiwa wewe kutokana na Mola wako Mlezi yatawazidishia wengi katika wao uasi na ukafiri. Basi usiwasikitikie watu makafiri.⁶⁸

69. Hakika walio amini, na Mayahudi na Masabii na Wakristo, walio muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya mwisho, na wakatenda mema, basi hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika.⁶⁹

70. Tulifanya agano na Wana wa Israili, na tukawatumia Mitume. Kila alipo wajia Mtume kwa wasio yapenda nafsi zao wengine waliwakanusha na wengine wakawauwa.⁷⁰

71. Na wakadhani kuwa hapatakuwa majaribio; basi wakawa vipofu na viziwi. Kisha Mwenyezi Mungu akawapokelea toba zao. Kisha tena wengi katika wao wakawa vipofu na viziwi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona hayo wayatendayo.⁷¹

72. Hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni Masihi mwana wa Maryamu! Na hali Masihi mwenyewe alisema: Enyi Wana wa Israili! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru.⁷²

73. Kwa hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa Utatu. Hali hakuna mungu ila Mungu Mmoja. Na ikiwa hawaachi hayo wanayo yasema, kwa yakini itawakamata adhabu chungu wale wanao kufuru.⁷³

68 Ewe Mtume! Waambie Watu wa Kitabu (yaani Biblia): Hakika nyinyi hamtakuwa mnafuata Dini sahihi ila mtapo zitangaza hukumu zote za Taurati na Injili na mkazitenda. Na mkaiamini Qur'ani iliyo teremshwa na Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kwa ajili ya kuwaongoa watu. Na yakinika, ewe Mtume, kwamba wengi wa Watu wa Kitabu watazidi udhalimu, na ukafiri, na inadi, juu ya Qur'ani kwa uhasidi wao na chuki. Basi usiwahuzunikie watu ambao wametiwa muhuri wa upinzani.

69 Hakika walio muamini Mwenyezi Mungu (yaani Waislamu), na wafwasi wa Musa katika Mayahudi, na walio toka kwenye dini nyenginezo, na wafwasi wa Isa katika Manasara - wote hao wakisafisha imani yao kwa Mwenyezi Mungu, na wakaamini kufufuliwa na malipo na wakatenda mema kama ilivyo funzwa na Uislamu, hao wote watasalimika na adhabu na watakuwa katika furaha ya Peponi Siku ya Kiyama.

70 Sisi tuliagana na Mayahudi, Wana wa Israili, kwa agano madhubuti katika Taurati kuwa wafuate hukumu zake. Na tukawapelekea Manabii wengi wawabainishie, na wawatilie mkazo ahadi yetu. Lakini walivunja ahadi. Wakawa kila akiwajia Mtume ambaye hakuwafikiana na matamania yao, ama walimkanusha au walimuuwa.

71 Na hao Wana wa Israili walidhani hawatapata majaribio, yaani shida za kuwafafanua baina ya walio simama imara na wasio simama imara. Kwa hivyo hawakuweza kustahamili, bali wengi wao walipotea wakawa kama vipofu na viziwi. Wakaiacha Haki, na Mwenyezi Mungu akawapatiliza kwa madhila. Baadae walipo rejea kwa Mwenyezi Mungu na wakatubu, alikubali toba zao, na akawarejeshea utukufu wao. Lakini baadae tena wakaingia katika upotofu, na wakawa kama vipofu na viziwi! Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema, na atashuhudia vitendo vyao, na atawalipa kwavyo.

72 Wenye kudai kuwa Mwenyezi Mungu yu katika Isa bin Maryam hata akawa yeye Mungu, kama wasemavyo Wakristo hii leo, hakika wamekufuru! Yeye Isa hana dhambi ya haya, kwani hakupata kudai hivyo hata mara moja. Bali yeye aliwaamrisha Wana wa Israili wamsafie imani Mwenyezi Mungu peke yake kwa kusema: Hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliye niumba mimi na nyinyi, na ndiye anaye niendeshea mambo yangu yote, na kwamba kila mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu malipo yake ni kuwa hatoingia Peponi kabisa, bali ataingia Motoni, kwa kuwa amekiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kuvunja mipaka yake hataepuka na adhabu. (Yesu kasema: "Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja." Marko 12.28. "Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe". Yohana 5.30 "Ninapaa kwenda kwa...Mungu wangu naye ni Mungu wenu." Yohana 20.17)

73 Haiwi mwenye kudai kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja katika Utatu, kama wadaivyo Wakristo sasa, awe anamuamini Mwenyezi Mungu!! Na hakika iliyo thibiti ni kuwa hapana mungu ila Mwenyezi Mungu mmoja pekee. Na ikiwa hawa walio potoka hawatoacha itikadi zao potovu, wakarejea kwenye

74. Je! Hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na wakamwomba msamaha? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu.⁷⁴

75. Masihi mwana wa Maryam si chochote ila ni Mtume. Wamekwisha pita Mitume kabla yake. Na mama yake ni mwanamke mkweli. Wote wawili walikuwa wakila chakula. Angalia jinsi tunavyo wabainishia Aya, kisha angalia vipi wanavyo geuzwa.⁷⁵

76. Sema: Je! Mnawaabudu, badala ya Mwenyezi Mungu, wale ambao hawawezi kukudhuruni wala kukufaeni? Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kujua.⁷⁶

77. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu bila ya haki. Wala msifuata matamania ya watu walio kwisha potea tangu zamani, na wakawapoteza wengi, na wenyewe wakapotea njia iliyo sawa.⁷⁷

78. Walilaaniwa walio kufuru miongoni mwa Wana wa Israili kwa ulimi wa Daud na wa Isa mwana wa Maryamu. Hayo ni kwa sababu waliasi na wakawa wanapindukia mipaka.⁷⁸

79. Walikuwa hawakatazani maovu waliyo kuwa wakiyafanya. Hakika ni maovu yalioje mambo waliyo kuwa wakiyafanya!⁷⁹

80. Utawaona wengi wao wanafanya urafiki na walio kufuru. Hakika ni maovu yaliyo

ut'iifu wa Mwenyezi Mungu, hapana budi ila itawasibu adhabu kali. (Biblia inasema kuwa ya kwanza katika Amri Kumi alizo pewa Musa ni: "Usiwe na miungu mingine ila mimi." - Kutoka 20.3. "Wewe umeonyeshwa haya, ili upate kujua ya kuwa Bwana ndiye Mungu, hapana ila yeye." - Kumbukumbu la Torati 4.35. Katika Injili ya Yohana 17.3 Yesu anamsemeza Mwenyezi Mungu: "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma").

74 Je! Watu hawa hawaziachilii mbali hizo itikadi za uzushi na uwongo, wakarejea kwenye Imani ya Mwenyezi Mungu, na wakaomba wafutiwe dhambi zao walizo zitenda? Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa maghfira, Mwingi wa rehema.

75 Isa bin Maryamu si chochote ila ni mwanaadamu aliye pata neema ya Mwenyezi Mungu kwa kuteuliwa kuwa ni Mtume kama walivyo mtangulia wengi kabla yake. Na Mama yake Isa ni mmoja katika wanawake, aliye jaaliwa kuwa ni mkweli katika kauli yake na mwenye kumuamini Mola wake Mlezi. Na yeye na mwanawe, Isa, walikuwa wana mahitajio yanayo hitajiwa na kila mwanaadamu, kama kula na kunywa, na kwenda haja. Na hizo ni dalili za ubinaadamu wao. Basi hebu zingatia, ewe mwenye kusikia, hali ya hao walio ingia upofu hata hawaoni dalili za Ishara zilizo wazi ambazo amewabainishia Mwenyezi Mungu. Tena zingatia vipi wanaiacha Haki juu ya kuwa ni iwazi kabisa

76 Ewe Mtume! Waambie hawa wapotovu: Vipi mnamuabudu mungu asiye weza kukudhuruni kwa lolote mkiacha kumuabudu, wala havezi kukufaeni kwa lolote mkimuabudu!! Vipi mnaacha kumuabudu Mwenyezi Mungu ambaye Yeye ndiye Mungu Mwenye uweza wa kila kitu, naye ni Mwenye kusikia, na Mwenye ujuzi.

77 Ewe Mtume! Waambie Watu wa Kitabu, yaani Mayahudi na Wakristo: Mwenyezi Mungu anakukatazeni msivuke mipaka katika itikadi zenu hata mkaingia katika upotovu, mkawafanya baadhi ya viumbe vyake kuwa ni miungu; au mkakanusha ujumbe wa baadhi ya Mitume. Na anakukatazeni kufuata matamania ya watu walio kutangulieni, walio acha njia ya uwongofu, na wakawazuia watu wengi kuifuata njia hiyo, na wakaendelea katika kuiepuka Njia ya Haki.

78 Mwenyezi Mungu amewatenga mbali na rehema yake wale makafiri miongoni mwa Wana wa Israili, na haya yameteremka katika Zaburi juu ya Nabii wake Daud, na katika Injili juu ya Nabii wake Isa mwana wa Maryam. Na hayo ni kwa sababu ya uasi wao, kutokana na ut'iifu wa Mwenyezi Mungu na kuzama kwao katika udhalimu na ufasadi. (Katika Zaburi Daud anawaapiza Mayahudi: "Wewe, Mungu, uwapatilize. Na waanguke kwa mashauri yao, Uwatoe nje kwa ajili ya wingi wa makosa yao, kwa maana wamekuasi Wewe." - Zaburi 5.10. Katika Injili Yesu anawalaani: "Enyi nyoka, wana wa majoka, mtaikimbiaje hukumu ya jehannum?" - Mathayo 23.33.)

79 Mtindo wao ulikuwa kutoambizana. Hapana amkatazaye mwenzie kufanya uovu. Kufanya kwao uovu na kuacha kukatazana ni katika vitendo vinavyo chusha mno.

tangulizwa na nafsi zao hata Mwenyezi Mungu amewakasirikia, nao watadumu katika adhabu.⁸⁰

81. Na lau wangeli kuwa wanamuamini Mwenyezi Mungu, na huyu Nabii, na yaliyo teremshwa kwake, wasingeli wafanya hao marafiki. Lakini wengi katika wao ni wapotofu.⁸¹

82. HAKIKA utawakuta walio shadidi kuliko watu wote katika uadui kwa walio amini ni Mayahudi na washirikina. Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanao sema: Sisi ni Manasara. Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki, na kwa sababu wao hawafanyi kiburi.⁸²

83. Na wanapo sikia yaliyo teremshwa kwa Mtume utaona macho yao yanachururika machozi kwa sababu ya Haki waliyo itambua. Wanasema: Mola wetu Mlezi! Tumeamini. Basi tuandike pamoja na wanao shuhudia.⁸³

84. Na kwa nini tusimuamini Mwenyezi Mungu na Haki iliyo tujia, na hali tunatumai Mola wetu Mlezi atuingize pamoja na watu wema?⁸⁴

85. Basi Mwenyezi Mungu atawalipa, kwa yale waliyo yasema, Bustani zipitazo mito katika yake; humo watadumu. Na haya ndiyo malipo ya wafanyao wema.⁸⁵

86. Na wale walio kufuru na wakazikanusha Ishara zetu, hao ndio watu wa Motoni.⁸⁶

87. Enyi mlio amini! Msiharimishe vizuri alivyo kuhalalishieni Mwenyezi Mungu,

80 Utawaona wengi miongoni mwa Wana wa Israili hufanya urafiki na washirikina, mapagani, na wanawafanya hao ndio wenzi wao wakishirikiana katika kuupiga vita Uislamu! Kitendo hichi kiovu wanajirimbikizia wenyewe nafsi zao, waje kupata malipo yake kwa kupata ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na wapate kudumu milele katika adhabu ya Jahannamu.(Hayo yalikuwa zama za Mtume s.a.w. na mpaka hii leo. Mayahudi wanatafuta kila rafiki ambaye atauvunja Uislamu, ilhali yafaa wawaone Waislamu ndio wa karibu mno nao, kwa kuwa wanaamini Mungu Mmoja na wanaamini Manabii wao wote.)

81 Na lau kuwa itikadi yao ni sawa kama inavyo faa iwe kwa kumuamini Mwenyezi Mungu, na Mtume wake Muhammad s.a.w., na Qur'ani aliyo teremshiwa, basi wasingeli wafanya makafiri kuwa ni wenzao kuwapinga Waumini. Lakini wengi miongoni mwa Wana wa Israili ni maasi, wameacha dini.

82 Ewe Nabii! Tunakuhakikishia ya kwamba utaona hapana watu wanao kuchukua na kukubughudhi wewe na wanao kuamini kama Mayahudi na hawa wanao mshirikisha Mwenyezi Mungu katika ibada. Na utawakuta walio karibu mno nawe kwa mapenzi ni wafwasi wa Isa, walio jiita wenyewe "Manasara". Kwa sababu wamo miongoni mwao makasisi wanao ijua dini yao, na marahibu (mamonaki) wat'awa, wanao mcha Mola Mlezi, na kuwa wao hawana kiburi cha kuwazuia wasisikie Haki. (Na haya yameonakana kuwa Waislamu wengi duniani asili yao walikuwa Manasara, Wakristo. Wao wakisha pata fursa ya kuufahamu Uislamu huufuata, lakini ni wachache miongoni mwa Mayahudi walio silimu. Kinacho wazuia ni kiburi. Lakini walio silimu basi wamekuwa Waislamu wakubwa.)

83 Na pia miongoni mwa Manasara wakiisikia Qur'ani aliyo teremshiwa Mtume huathirika nayo, macho huwatiririka machozi, kwa kuwa wanajua kuwa wanayo yasikia ni kweli tupu, basi nyoyo zao humili kwayo, na ndimi zao huomba dua kumwomba Mwenyezi Mungu kwa kusema: Mola wetu Mlezi! Tumekuamini Wewe na Mitume wako, na Haki ulio wateremshia. Basi ipokee Imani yetu, na utufanye miongoni mwa Umma wa Muhammad ulio wafanya mashahidi na hoja kwa watu wote Siku ya Kiyama.

84 Na nini cha kutuzuia tusimsadiki Mwenyezi Mungu peke yake, na Haki iliyo teremka kwa Muhammad? Na hali sisi tunamtaraji Mwenyezi Mungu atuingize Peponi pamoja na watu wenye Imani njema na vitendo vyema.

85 Kwa hivyo Mwenyezi Mungu amewaandikia malipo kwa vile kuungama kwao, nayo ni Bustani yenye kupita mito chini ya miti yake, na majumba ya fakhari ya kukaa humo daima, pamoja na watu ambao ni njema itikadi zao na vitendo vyao.

86 Na walio mpinga Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wakazikanya dalili alizo wateremshia kuwa ni uwongofu wa kufikia Haki, ni wao peke yao wanao stahiki adhabu kali katika Jahannamu.

wala msikiuke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wakiukao mipaka.⁸⁷

88. Na kuleni katika alivyo kuruzukuni Mwenyezi Mungu, halali na vizuri. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mnamuamini.⁸⁸

89. Mwenyezi Mungu hatakushikeni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini atakushikeni kwa mnavyo apa kweli kweli kwa makusudio. Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnacho walisha ahali zenu, au kuwavisha, au kumkomboa mtumwa. Asiye pata hayo, basi afunge siku tatu. Hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapo apa. Na hifadhini yamini zenu. Namna hivyo Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake ili mpate kushukuru.⁸⁹

90. Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shet'ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa.⁹⁰

91. Hakika Shet'ani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mmeacha?⁹¹

92. Na mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume, na tahadharini. Na ikiwa mtageuka basi jueni ya kuwa juu ya Mtume wetu ni kufikisha ujumbe tu ulio wazi.⁹²

87 Enyi mlio amini! Msijiharimishie nafsi zenu vitu vizuri alivyo kuhlalishieni Mwenyezi Mungu, wala msipite mipaka aliyo kuwekeeni Mwenyezi Mungu ya kufuata mambo ya wastani. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi watu wanao pindukia mipaka.

88 Na kuleni vitu alivyo kupeni Mwenyezi Mungu na akavifanya vyepezi kwenu, na akavifanya ni halali na ni vizuri kwa nafsi zenu. Na daima mwogopeni Mwenyezi Mungu, na mt'iini Yeye maadamu nyinyi mnamuamini Yeye

89 Mwenyezi Mungu hakutiini adabu kwa sababu ya kuapa kiapo msicho kusudia. Bali hakika Yeye hukutieni adabu kwa sababu ya kuvunja viapo mlivyo vikusudia na yamini mliyo jifunga nayo. Basi ikiwa mmevunja kiapo itakupaseni mfanye jambo la kukughufirieni dhambi zake. Na mambo yenyewe ni: kuwalisha mafakiri kumi kwa siku moja, kwa chakula cha kawaida mnacho kila nyinyi na jamaa zenu mnao waangalia, yaani watu wenu wa nyumbani bila ya israfu wala ubakhili. Au kuwavika mafakiri kumi kwa kivazi kilicho zowewa. Au kumkomboa mtu kutoka utumwani. (Na mfano wa mtumwa ni mtu alioko kifungoni kwa dhulma, au chini ya utawala wa dhulma.) Ikiwa mwenye kuapa hawezi kutenda lolote katika hayo, basi itampasa afunge siku tatu. Na kila moja katika mambo haya hufuta dhambi za mwenye kuapa kiapo cha kutilia niya na akakivunja. Nanyi zilideni yamini zenu, msiape katika mambo yasiyo kuwa laiki yake, na wala msiache kutenda kitendo cha kughufiria dhambi pindi mkivunja kiapo. Kwa mpango huu Mwenyezi Mungu anakufafanulieni hukumu zake ili mpate kushukuru neema zake kwa kujijua na kuzifuata vilivyo. (Tazama Maelezo 5:89)

90 Enyi wenye kumsadiki Mwenyezi Mungu na Vitabu vyake na Mitume wake, wenye kuifuata Haki! Kunywa au kuvuta chochote kinacho leweshwa, kucheza kamari, na kusimamisha mawe ya kutolea mihanga kwa ajili ya masanamu mnayo yaabudu, na kuagua kwa mishale, na mawe, na karatasi za kuagulia kudra iliyo ghaibu...yote hayo si chochote ila ni uchafu wa kiroho, na upotovu. Na hayo ni kupambiwa na Shetani tu. Basi yaachilieni mbali ili mpate kufuzu duniani kwa maisha bora, na Akhera mpate Janna yenye neema. (Tazama Maelezo 5:90)

91 Bila ya shaka Shetani hana atakalo kwa kukushawishini kunywa ulevi na kucheza kamari ila kuleta khitilafu na ugomvi na kuchukiana baina yenu ili mdhoofike kwa kuondoka masikizano, na uvunjike umoja wenu, kwa sababu anavyo kukupendeleeni mnywe ulevi na mcheze kamari. Na hayo ili mpate kuacha kumuabudu Mwenyezi Mungu, na muache Sala, ili Akhera yenu iwe ova kama ilivyo dunia yenu. Basi jee! Baada ya nyinyi kujua maovu haya hamyatupilii mbali ninayo kukutazeni, mkamkosesha Iblisi makusudio yake. (Tazama Maelezo 5:91)

92 Na fuateni amri ya Mwenyezi Mungu na amri ya Mtume wake kwa yale anayo kuleteeni kutoka kwa Mola wake Mlezi. Na yaepukeni mbali yatakayo kuleteeni adhabu mnapo kwenda kinyume. Mkitofuata anayo kuamrisheni Mwenyezi Mungu kuweni na yakini kuwa Yeye atakupeni adabu. Wala nyinyi hamna udhuru wowote baada ya kuwa Mtume amekwisha wabainishieni adabu ya kupewa wakhalifu. Na hakika haimpasi Mtume wetu ila kukujuyeni hukumu zetu tu, na kukubainishieni kwa ukamilifu wa uwazi.

93. Si dhambi juu ya walio amini na wakatenda mema kwa walivyo vila (zamani) maadamu wakichamngu na wakiamini na wakitenda mema, kisha wakachamngu, na wakaamini, kisha wakachamngu na wakafanya mazuri. Na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao mazuri.⁹³

94. Enyi mlio amini! Mwenyezi Mungu atakujaribuni kidogo kwa wanyama wa kuwinda inayo wafikia mikono yenu na mikuki yenu, ili Mwenyezi Mungu amjue nani anaye mkhofu kwa ghaibu. Basi atakaye ruka mipaka baada ya hayo atapata adhabu kali.⁹⁴

95. Enyi mlio amini! Msiue wanyama wa kuwinda nanyi mmeharimia katika Hija. Na miongoni mwenu atakaye muuwa makusudi, basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilicho sawa na alichu kiuwa, katika mifugo, kama wanavyo hukumu waadilifu wawili miongoni mwenu. Mnyama huyo apelekwe kwenye Al Kaaba, au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini; au badala ya hayo ni kufunga, ili aonje ubaya wa jambo lake hili. Mwenyezi Mungu amekwisha yafuta yaliyo pita; lakini atakaye fanya tena Mwenyezi Mungu atampa adhabu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu na Mwenye kuadhibu.⁹⁵

96. Nyinyi mmehalalishiwa kuvua vinyama vya baharini na kuvila, kwa faida yenu na kwa wasafiri. Na mmeharimishiwa mawindo ya wanyama wa bara maadamu mmeharimia Hija. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mtakusanywa kwake.⁹⁶

93 Walio mkubali Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakatenda mema, hawana dhambi kwa vyakula vya halali na vizuri wanavyo kula, wala vya haramu walivyo wahi kula zamani kabla hawajajua kuwa ni haramu, ikiwa wanamkhofu Mwenyezi Mungu na wakajitenga navyo vyakula hivyo baada ya kujua kuwa vinakatazwa. Kisha ikawa wao wakaendelea kumkhofu Mwenyezi Mungu na kuzikubali sharia zake, na kisha wakadumu katika khofu yao ya kumwogopa Mwenyezi Mungu katika kila hali, na wakawa wanafanya a'mali zao kwa usafi wa niya, na kwa njia ya ukamilifu. Kwani hakika Mwenyezi Mungu huwalipa wenye ikhlasi katika vitendo vyao kwa kadri ya ikhlasi yao na a'mali yao.

94 Enyi mlio amini! Hakika Mwenyezi Mungu anakufanyieni mtihani wakati wa Hija kwa kukuharimishieni baadhi ya wanyama na ndege ambao mnaweza kuwawinda kwa wepesi kwa mikono yenu na mikuki yenu. Makusudio ni kutaka wajuulikane ambao wanamt'ii Mwenyezi Mungu ijapo kuwa hawaonekani na watu. Na wanao pindukia mipaka aliyo iweka Mwenyezi Mungu baada ya kuibainisha watakuja pata adhabu kali.

95 Enyi ambao mmeamini! Msiuwe nyama wa kuwinda nanyi mmenuia Hija na Umra na mmo kuzitimiliza. Na mwenye kumuua mnyama kama huyo kwa kukusudia basi itampasa atoe fidiya mfano wa mnyama aliye muuwa, ikiwa katika ngamia, ng'ombe au kondoo. Na hujuulikana huyo mfano wake kwa kukadiriwa na watu wawili waadilifu kati yenu, wahukumu na wawape mafakiri kwenye Al Kaaba, au atoe badala yake awape, au atoe chakula kadiri ya yule mnyama kuwapa mafakiri. Kila fakiri apewe chakula cha kumtoshia kutwa yake. Hayo ndio kuondoa dhambi za kuwinda kuliko katazwa. Au badala ya hayo yote, afunge idadi ya siku za kadri ya wale masikini iliyo mbidi kuwalisha lau angewalisha. Na Mwenyezi Mungu amelazimisha hayo ili huyo mwenye kufanya lile kosa apate kuhisi matokeo ya kosa lake na uwovu wa malipo yake. Mwenyezi Mungu, lakini, amesamehe ukhalifu ulio tendelea kabla ya jambo hilo halijaharimishwa. Na mwenye kurejea tena kufanya uovu baada ya kujua kuwa ni haramu, basi hakika Mwenyezi Mungu atampa adabu kwa kitendo chake, naye Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushinda hashindiki, Mkali wa kumuadhibu anaye kakamia kutenda dhambi. (Tunaona kuwa Uislamu ulianzisha kulinda mazingara, na utajiri wa asili tangu hapo kale. Kutokana na kuhifadhiwa wanyama na ndege wa porini huko Makka, ndio hii leo tunaona zipo nyanda na mapori yanayo hifadhiwa wanyama wake, kwa mujibu wa utaalumu wa kisasa.)

96 Mwenyezi Mungu amekuhalalishieni kuvua wanyama wa baharini, na muwale, na wanufaike kwao wakaazi wenyeji na wasafiri. Na amekuharimishieni kuwinda wanyama wa bara wasio fugwa kwa kawaida majumbani, katika muda ule unapo kuwa katika Hija au Umra, kwenye eneo takatifu linalo itwa Alharam. Na mzingatieni Mwenyezi Mungu, na iogopeni adhabu yake. Basi msende kinyume naye,

97. Mwenyezi Mungu amefanya Al Kaaba, hii Nyumba Tukufu, ni simamio la watu, na kadhaalika Miezi Mitukufu, na wanyama wa dhabihu, na vigwe. Hayo ili mjue ya kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo katika ardhi, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.⁹⁷

98. Jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira, na Mwenye kurehemu.⁹⁸

99. Haimlazimu Mtume ila kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu anajua mnacho kidhihirisha na mnacho kificha.⁹⁹

100. Sema: Haviwi sawa viovu na vyema ujapo kupendeza wingi wa viovu. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili, ili mpate kufanikiwa.¹⁰⁰

101. Enyi mlio amini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni. Na mkiyauliza inapo teremshwa Qur'ani mtabainishiwa. Mwenyezi Mungu amesamehe hayo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira Mpole.¹⁰¹

102. Waliyauliza hayo watu wa kabla yenu, kisha wakawa wenye kuyakataa.¹⁰²

103. Mwenyezi Mungu hakujaalia uharamu wowote juu ya "*Bahira*" wala "*Saiba*" wala "*Wasila*" wala "*Hami*". Lakini walio kufuru humzulia uwongo Mwenyezi

kwani nyinyi mtarejea kwake Siku ya Kiyama, na hapo atakulipeni kwa yote mliyo yatenda. (Huu ni mfano katika mifano mingi ya Uislamu tangu hapo kale unavyo pendelea kulinda tabia ya mazingara kwa kuhifadhi wanyama wasiuliwe ovyo, na miti isikatwe ovyo, na hata maji ya mito na maziwa yasitumiwe kwa fujo, kwani Mwenyezi Mungu hawapendi wafujaji!)

97 Mwenyezi Mungu ameiijaalia Al Kaaba, nayo ni hiyo nyumba aliyi itukuza na akaharimisha watu na wanyama kufanyiwa uadui ndani yake na karibu yake, ameiijaalia kuwa yenye kusimama na yenye kutukuzwa, na yenye kuwapa amani watu, na iwe ndiyo Kibla cha kuelekea watu katika Sala zao, na watu waiende kwa Hija wawe ni wageni wa Mwenyezi Mungu, na ili watende yale ya kuupa nguvu umoja wao. Hali kadhaalika ameufanya mwezi wa Hija na wanyama wanao tolewa dhabihu, na khasa wale wanao vishwa vigwe ili watambuliwe na wanao waona kuwa hao wametolewa hidaya kwenye hiyo Nyumba. Na natija ya kuweka yote hayo ni kuwa mpate kuyakinika kuwa ujuzi wake Mwenyezi Mungu umeenea kila kitu kililo mbinguni kunakotoka wahyi (ufunuo) wa sharia, na umeenea duniani, anako weka sharia ya kuwaletea watu maslaha yao. Na hakika ujuzi wa Mwenyezi Mungu umeenea juu ya kila kitu.

98 . Enyi watu! Jueni kuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali, humteremkia anaye halalisha vya haramu, naye pia ni Mwingi wa kusamehe dhambi za mwenye kutubu na akaingia kumt'ii. Naye ni Mwenye rehema sana, na kwa hivyo hamchukulii mtu papo kwa papo kwa kila alitendalo.

99 Haimlazimikii Mtume ila kuwafikishia watu anayo funuliwa yeye, ili isimame hoja juu yao na wasiwe na kisingizio chochote cha kuwa ati hawakuonywa wala hawakufunzwa. Basi yajueni anayo kuleteeni Mtume, kwani Mwenyezi Mungu anayajua mnayo dhihirisha na mnayo yaficha.

100 Ewe Nabii! Waambie watu: Si sawa sawa vile vizuri anavyo kuhalalishieni Mwenyezi Mungu na vibaya anavyo kuharimishieni. Kwani farka iliyo baina ya viwili hivyo kwa Mwenyezi Mungu ni kubwa, na hata hivyo vibaya vingawa ni vingi na vinawapendeza watu wengi. Basi enyi wenye akili! Ufanyeni ut'iifu kwa Mwenyezi Mungu uwe ni kinga yenu isikupateni adhabu yake kwa kukhiari vilivyo vyema, na kujepusha na viovu, ili mpate kuwa miongoni walio fuzu duniani na Akhera.

101 Enyi mlio amini! Msimuulize Nabii mambo ambayo Mwenyezi Mungu amekuficheni mkataka yafichuliwe, na mkamuuliza Nabii katika uhai wake, kwani Qur'ani inamteremkia bado. Na Mwenyezi Mungu atakubainishieni itapo hitajika. Mwenyezi Mungu amekusameheni kwa yasiyo tajwa, hatokuadhibuni kwayo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, na Mwenye wasaa katika upole. Basi hana papara katika kuadhibu.

102 Katika jamaa walio kutangulieni walikuwapo walio uliza mfano wa haya, mambo mazito mazito; na Manabii wao walipo wakalifisha ya kufanya wakaona mazito kuyatenda, wakayaacha, na wakawa ni wenye kuyakanya. Kwani Mwenyezi Mungu hupendelea wepesi, wala hapendelei uzito; na huwkalifisha watu kwa wanayo yaweza.

Mungu, na wengi wao hawatunii akili.¹⁰³

104. Na wanapo ambiwa: Njooi kwenye yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, na kwa Mtume, husema: Yanatutosha tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka?¹⁰⁴

105. Enyi mlio amini! Kilicho lazima juu yenu ni nafsi zenu. Hawakudhuruni walio potoka ikiwa nyinyi mmeongoka. Ni kwa Mwenyezi Mungu ndio marudio yenu nyote; basi atakwambieni yale mliyo kuwa mkiyatenda.¹⁰⁵

106. Enyi mlio amini! Yanapo mfikia mauti mmoja wenu na akataka kutoa wasia, basi wawepo mashahidi wawili miongoni mwenu ambao ni waadilifu. Na mnapo kuwa safarini, na msiba wa mauti ukakusibuni, basi washuhudie wengineo wawili wasio kuwa katika nyinyi. Mtawazuia wawili hao baada ya Sala na waape kwa Mwenyezi Mungu, mkitilia shaka, wakisema: Hatutopokea thamani yoyote kwa haya hata kwa ajili ya jamaa; na wala hatutaficha ushahidi wa Mwenyezi Mungu; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye dhambi.¹⁰⁶

107. Ikgundulikana kuwa wawili hao wamestahiki dhambi, basi wawili wengineo kutokana na warithi wenye kudai haki washike makamo ya wa mwanzo. Nao waape kwa Mwenyezi Mungu wakisema: Hakika ushahidi wetu ni wa haki zaidi kuliko ushahidi wa wale. Na sisi hatujafanya dhambi; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa walio dhulumu.¹⁰⁷

103 Mwenyezi Mungu hakukupeni ruhusa kuharimisha kitu alicho kuhalalishieni, na kwa hivyo mkenda mkawapasua ngamia masikio yao, na mkajizua kuwatumia mkawaita “Bahira” mkawawacha kwa kuwekea nadhiri, na mkawaita “Saiba”; na mkaharimisha kula kondoo dume, na mkawatoa kuwa tunza kwa masanamu; na hata kondoo akizaa dume na jike mkamwita “Wasila”, na mkakataa kumchinja dume lake. Wala Mwenyezi Mungu hakukufanyieni sharia ya kukuharimishieni msimtumie ngamia dume baada wakisha zalikana kutokana naye matumbo kumi, naye mkamwita “Hami”! Mwenyezi Mungu hakukutungieni sharia yoyote ya namna hiyo. Lakini walio kufuru wanazua uwongo na wanamsingizia Mwenyezi Mungu. Na wengi wao hawatunii akili. (*Tazama Maelezo 5:103*)

104 Na hawa makafiri wakiambiwa: Njooi kwenye yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu katika Qur’ani, na aliyo yaeleza Mtume, ili mpate kuongoka kwa kuyafuata, wao husema: Yanatutosha tuliyo wakuta nayo baba zetu. Yawafalia hawa kusema hayo? Ijapo kuwa hao baba zao ni kama nyama hoa, hawajui lolote la haki, wala hawajui njia ya kuenda yaliyo sahihi.

105 Enyi mlio amini! Fanyeni pupa ya kwenda kwenye matengenezo ya nafsi zenu kwa kumt’ii Mwenyezi Mungu. Upotovu wa mwengineo hautakudhuruni ikiwa nyinyi mmo kwenye uwongofu na mnalingania Haki. Na nyote nyinyi marejeo yenu ni Mwenyezi Mungu peke yake Siku ya Kiyama. Hapo atakupeni khabari ya vitendo vyenu, na kila mmoja wenu atamlipa kwa aliyo yatanguliza, na wala hapana hata mmoja atae shikwa kwa dhambi za mwengineo.

106 Enyi mlio amini! Mmoja wenu anapooa alama za kukaribia mauti na akataka kuusia lolote basi kushuhudia wasia huo iwe: kushuhudia watu wawili waadilifu katika jamaa zenu, au watu wawili wengineo ikiwa mmo safarini na ishara za mauti zikatokea. Wazuieni wawili hao baada ya Sala wanapo kusanyika watu, na waape kwa jina la Mwenyezi Mungu wakisema: Hatubadilishi kwa kiapo chake kwa chochote, hata ikiwa ni kutufaa sisi au yeyote katika jamaa zetu. Wala hatutaficha ushahidi alio tuamrisha Mwenyezi Mungu kuutimiza baraabara. Kwani tukificha ushahidi au tukasema lisio la kweli, tutakuwa miongoni mwa wenye kudhulumu na kustahiki adhabu ya Mwenyezi Mungu.

107 Na ikionekana kuwa mashahidi wawili hao wamesema uwongo katika ushahidi wao, au wameficha kitu, basi walio na haki zaidi kushika mahala pao ni wawili wengine walio karibu zaidi kukhusika na warithi wa maiti. Hao washike pahala pao baada ya Sala, wadhahirishe uwongo wa walio tangulia, na waape kwa Mwenyezi Mungu kuwa wale mashahidi wa mwanzo walisema uwongo, na: Yamini yetu inafaa zaidi kuliko yamini ya wale, na wala hatuitupi haki katika yamini zetu, wala hatuwatumu mashahidi wale kwa uzushi. Kwani tukifanya hivyo tutakuwa katika walio dhulumu, wenye kustahiki adhabu ya mwenye kumdulumu mwengineo.

108. Hivi inaelekea zaidi ya kwamba watatoa ushahidi ulio sawa au wataogopa visije vikaletwa viapo vingine baada ya viapo vyao. Na mcheni Mwenyezi Mungu na msikie. Na hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi wapotofu.¹⁰⁸

109. Ile siku ambayo Mwenyezi Mungu atapo wakusanya Mitume awaambie: Mlijibiwa nini? Watasema: Hatuna ujuzi; hakika Wewe ndiye Mjuzi Mkubwa wa yote yaliyo fichikana.¹⁰⁹

110. Na pale Mwenyezi Mungu atapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Kumbuka neema yangu juu yako, na juu ya mama yako, nilipo kutia nguvu kwa Roho Takatifu, ukazungumza na watu katika utoto na utuuzimani. Na nilivyo kufunza kuandika na hikima na Taurati na Injili. Na ulipo tengeneza udongo sura ya ndege, kwa idhini yangu, kisha ukapuliza ikawa ndege kwa idhini yangu; na ulipo waponesha vipofu na wakoma kwa idhini yangu; na ulipo wafufua wafu kwa idhini yangu; na nilipo kukinga na Wana wa Israili ulipo wajia na hoja zilizo wazi, na wakasema walio kufuru miongoni mwao: Haya si lolote ila ni uchawi mtupu!¹¹⁰

111. Na nilipo wafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume wangu, wakasema: Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu.¹¹¹

112. Wanafunzi walipo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Je, Mola wako Mlezi anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni? Akasema: Mcheni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini.¹¹²

108 Hukumu hii ndiyo njia ya karibu mno ya kuwezesha mashahidi watoe ushahidi ulio sawa kwa kuhifadhi kiapo chao kwa Mwenyezi Mungu, au kwa kuogopa kufedheheka kwa kudhihiri uwongo wao, pindi ikiwa warithi watakula yamini kupinga kiapo chao. Nanyi mumuangalie sana Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu na amana zenu, na zit'iini hukumu zake, na muwe radhi nazo. Kwani katika hayo ndiyo yanapatikana maslaha yenu. Na msikhalifu hukumu za Mwenyezi Mungu, msije kutoka kwenye ut'iifu wake, kwani Yeye hamnafishi kwa uwongozi wake mwenye kutoka katika ut'iifu wake.

109 Nanyi ikumbukeni Siku ya Kiyama pale Mwenyezi Mungu atapo wakusanya mbele yake Mitume wote akawauliza: Hao kaumu zenu niliyo kutumeni kwao wamekujibuni nini? Waliamini au walikanya? Na hao kaumu wakati huo watakuwa wamehudhuria ili hoja iwe juu yao kwa ushahidi wa Mitume wao wakisema: Hakika sisi hatujui yaliyo tokea baada yetu kwa hao ulio tupeleka kwao. Ni Wewe peke yako ndiye unaye jua hayo, kwa kuwa Wewe ndiye uliye kusanya ujuzi wa vilivyo fichikana kama unavyo jua vilivo dhaahiri.

110 Na wakati huo, Mwenyezi Mungu atamwambia Isa mwana wa Maryamu miongoni mwa Mitume: Kumbuka neema niliyo kuneemesha wewe na mama yako katika dunia, nilipo kutia nguvu kwa Wahyi,(Ufunuo), na nikakutamkisha nawe ni mtoto mchanga ili kumuondolea tuhuma aliyotehumiwa mama yako, kama nilivyo kutamkisha nawe ni mtu mzima kwa ufunuo niliyo kufunulia; na nilipo kuneemesha kwa kukufunza kuandika, na nikakuwezesha kusema na kutenda yaliyo sawa, na nikakufunza Kitabu cha Musa na Injili niliyo kuteremshia wewe, na nikakuwezesha kutenda miujiza asiyo weza mtu mwingine kuitenda, ulipo tengeneza ndege kwa udongo kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, ukapuliza akawa ndege aliye hai kwa uweza wa Mwenyezi Mungu, si kwa uweza wako, na ukamponesha mtoto kipofu, na ukamponesha mkoma kwa idhini na uweza wa Mwenyezi Mungu, na yakawa kwa kupitia mikononi mwako makadara ya kufufuka maiti kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na kudra yake, na pale nilipo wazuia Mayahudi wasikuuwe na kukusalibu nilipo waletea miujiza wapate kuamini, nao baadhi yao walikanya na wakadai kuwa hiyo miujiza si lolote ila ni dhaahiri uchawi tu. (Katika Injili ya Luka inasemwa "Malaika kutoka mbinguni akamtokea akamtia nguvu." Luka 22.43. Na katika Injili ya Yohana 5.30 Yesu anakiri: "Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe.")

111 Ewe Mtume! Watajie umma wako yaliyo tokea tulipo watia hima kikundi cha alio wataka Isa wamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake Isa, na wakamuitikia wakawa ndio Wanafunzi wake makhsusi, na wakasema: Tumeamini. Na shuhudia ewe Mola wetu Mlezi, kuwa sisi tumesafi niya zetu, na tunafuata amri zako, yaani Waislamu.

112 Ewe Nabii! Taja pia yaliyo tokea pale wafuasi wa Isa wenye ikhlasi walipo sema: Ewe Isa bin

113. Wakasema: Tunataka kukila chakula hicho, na nyoyo zetu zitue, na tujue kwamba umetuambia kweli, na tuwe miongoni mwa wanao shuhudia.¹¹³

114. Akasema Isa bin Maryamu: Ewe Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wetu! Tuteremshia chakula kutoka mbinguni ili kiwe Sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe ni Ishara itokayo kwako. Basi turuzuku, kwani Wewe ndiye mbora wa wanao ruzuku.¹¹⁴

115. Mwenyezi Mungu akasema: Hakika Mimi nitakuteremshieni hicho. Lakini yeyote katika nyinyi atakaye kanya baadae, basi hakika Mimi nitampa adhabu nisiyopata kumpa yeyote katika walimwengu.¹¹⁵

116. Na pale Mwenyezi Mungu atakapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu? (Na Isa) atasema: Subhanaka, Wewe umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa nilisema basi bila ya shaka umekwisha yajua. Wewe unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yaliyo katika nafsi yako. Hakika Wewe ndiye Mjuzi mkubwa wa yaliyo fichikana.¹¹⁶

117. Sikuwaambia lolote ila uliyo niamrisha, nayo ni: Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipo kuwa nao. Na ulipo nifisha ukawa Wewe ndiye Muangalizi juu yao. Na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu.¹¹⁷

118. Ukiwaadhibu basi hao ni waja wako. Na ukiwasamehe basi Wewe ndiye Mwenye nguvu na Mwenye hikima.¹¹⁸

Maryamu! Hivyo Mola wako Mlezi atakuitikia ukimtaka akuteremshie chakula kutoka mbinguni? Isa akawaambia kuwajibu: Kama nyinyi ni kweli mnamuamini Mwenyezi Mungu, basi mkhofuni Yeye, na fuateni amri zake na makatazo yake. Wala msitafute hoja ila nilizo kuleteeni.

113 Wakasema: Hakika sisi tunataka kula katika chakula hicho, ili nyoyo zetu zitue kwa kudra ya Mwenyezi Mungu tunayo iamini, na tujue kwa kuona kwa macho ya kuwa hakika ni kweli hayo unayo twambia yanatoka kwake *Subhanahu*, Aliye takasika, na tupate kutoa ushahidi kwa muujiza huu kwa hao ambao hawakuuona.

114 Isa akawaitikia, na akasema: Ewe Mola wetu Mlezi, uliye miliki mambo yetu yote! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni, kiwe ni siku-kuu kwetu kitapo teremka kwa walio amini miongoni mwetu, kwa walio tangulia na walio taakhari, na kiwe ni muujiza wa kutilia nguvu wito wako, na uturuzuku riziki njema, na Wewe ndiye Mbora wa kuruzuku.

115 Mwenyezi Mungu akamwambia: Mimi nitakuteremshieni chakula kutoka mbinguni. Lakini mtu yeyote atakaye pinga neema hii baada ya kuteremka, basi Mimi nitampa adabu ambayo sijapata kumpa mtu yeyote. Kwani huyo atakuwa anakanya baada ya kwisha shuhudia dalili ya Imani aliyote itaka mwenyewe.

116 Ewe Nabii! Taja yatakayo tokea Siku ya Kiyama, Mwenyezi Mungu atapo mwambia Isa bin Maryamu kauli ya kutangaza haki: Ati wewe ndiye uliye waambia: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu, na muache kumuabudu Mwenyezi Mungu wa pekee? Isa atasema: Mimi ninakutakasa mtakaso wa ukamilifu ya kuwa Wewe huna mshirika. Wala hainifalii mimi nitake jambo ambalo sina haki nalo hata chembe. Lau kuwa nimesema hayo, basi Wewe ungesi jua. Kwani Wewe unayajua yaliyo fichikana ndani ya nafsi yangu, licha yanayo dhihiri kwa kuyasema. Wala mimi siyajui unayo nificha. Hakika Wewe ndiye Mwenye ujuzi ulio enea kila kilicho fichikana na kilicho ghibu. (Wakristo wote wanamuabudu Yesu, na Wakatoliki wanamwomba Maryamu pia, na wanamwita: "Mama wa Mungu".)

117 Mimi sikuwaambia ila uliyo niamrisha niwafikishie. Nimewaambia: Muabuduni Mwenyezi Mungu peke yake. Kwani Yeye ndiye Mwenye kumiliki mambo yangu na yenu. Na mimi nilikuwa najua hali yao nilipo kuwa nao. Na ulipo malizika muda uliyo nikadiria nikae nao ulikuwa Wewe peke yako ndiye unaye wajua. Na Wewe ni Mwenye kujua kila kitu.

118 Ukiwaadhibu kwa waliyo yatenda basi hao ni waja wako, unawafanya upendavyo. Na ukiwasamehe, basi hakika Wewe peke yako ndiye Mtenda nguvu usiye shindwa, Mwenye hikima yenye kufikilia kila linalo toka kwako.

119. Mwenyezi Mungu atasema: Hii ndiyo Siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata Bustani zipitazo mito kati yake. Humo watadumu milele. Mwenyezi Mungu amewawia radhi, nao wawe radhi naye. Huku ndiko kufuzu kukubwa.¹¹⁹

120. Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo. Naye ni Muweza wa kila kitu.¹²⁰

119 Mwenyezi Mungu atasema: Hii ndiyo siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao. Watapata mabustani yanayo pitiwa na mito chini ya miti yake. Na humo watakaa, wala hawatatoka milele, wakistarehe humo kwa radhi ya Mwenyezi Mungu anavyo waridhia wao, na wao watavyo kuwa radhi kwa malipo alio walipa. Na Neema hiyo ndio kufuzu kukubwa.

120 Ufalme wa mbinguni na katika ardhi na vyote viliomo humo ni wa Mwenyezi Mungu peke yake. Yeye peke yake ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa, na Yeye tu ndiye Mwenye uweza ulio timia kutekeleza kila alitakalo.

Sura 6 - Al-An'am

Utangulizi

Sura hii ni ya Makka isipo kuwa Aya hizi: 20, 23, 91, 93, 114, 141, 151, 152, na 153. Na Aya zake ni 165. Iliteremka baada ya Sura Al-Hijr. Na Sura hii tukufu imekusanya maana zilizo wekwa mbali mbali kama ifuatavyo:

1. Imewazindua watu wauzingatie ulimwengu na dalili ziliomo ndani yake zenye kuonyesha Ubora wa aliye uumba, na Utukufu wake na Umoja wake wa pekee, na kuwa Yeye hashirikiani na yeyote, la katika kuumba, wala katika kuabudiwa, wala katika dhati yake.
2. Na imekusanya visa vya baadhi ya Manabii, na ikaanza kwa kisa cha Ibrahim a.s. kwa kubainisha kuwa alichukua maana ya ibada na Tawhidi kwa kuuchungua ulimwengu, na kufuata yaliyomo ndani yake. Naye alianza kwa kupeleleza nyota, kisha mwezi, kisha jua, na akamalizia kwa kufuata ibada ya Mwenyezi Mungu peke yake.
3. Na ikapelekea macho yaangalie ajabu za uumbaji na vipi mambo yanavyo kuwa. Ikbainisha vipi kilicho hai kinyevu kinatokana na kisicho kuwa na uhai kikavu; na vipi mbegu inavyo pasuka na ukachipua mmea.
4. Na Sura hii imezitaja sifa za wapinzani, na vipi wanavyo shikilia ndoto zao zinazo watenga na Haki, na zinazo wapotosha.
5. Na ndani ya Sura hii umebainishwa uhalali wa vyakula alivyo halalisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, na upotovu wa Washirikina walivyo jiharimishia wenyewe bila ya kutegemea dalili yoyote, na vipi wanavyo mnasibishia kuharimisha huko Mwenyezi Mungu Aliye Takasika.
6. Na ndani yake yamebainishwa mambo haya, ambayo ndio mukhtasari wa Uislamu na tabia njema za kusifika. Mambo yenyewe ni:- kuharimisha ushirikina, uzinzi, kuuwa mtu, kula mali ya yatima, waajibu wa kutimiza vipimo na mizani, kutimiza uadilifu, kutekeleza ahadi, kuwatendea wema wazazi, na kukataza kuwazika watoto wa kike nao wahai.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliye umba mbingu na ardhi, na akafanya giza na mwangaza. Tena baada ya haya walio kufuru wanawafanya wengine sawa na Mola wao Mlezi.¹
2. Yeye ndiye aliye kuumbeni kwa udongo, kisha akakuhukumieni ajali, na muda maalumu uko kwake tu. Tena baada ya haya nyinyi mnatia shaka.²

1 Kuhimidiwa, yaani kusifiwa na kutajwa kwa wema, ni kwa Mwenyezi Mungu aliye ziumba mbingu na ardhi, na akaumba, kwa kudra yake, giza na mwangaza, kwa manufaa ya waja wake, na kuambatana na hikima yake. Tena pamoja na neema zote hizi nzuri hawa makafiri wanakwenda mshirikisha Mwenyezi Mungu, na wakawafanya wengineo ni washirika wa Mwenyezi Mungu katika ibada!! (*Tazama Maelezo 6:1*)

2 Yeye Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuanzeni kwa kukuumbeni kutokana na udongo. Kisha akamkadiria

3. Na Yeye ndiye Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhini. Anajua ya ndani yenu na ya nje yenu. Na anajua mnayo yachuma.³
4. Na haiwafikii hata ishara moja katika ishara za Mola wao Mlezi ila wao huwa wenye kuipa nyongo.⁴
5. Wameikanusha Haki ilipo wajia. Basi zitawajia khabari za yale waliyo kuwa wakiyakejeli.⁵
6. Jee, hawaoni vizazi vingapi tulivyo viangamiza kabla yao? Tuliwaweka katika nchi tusivyo kuwekeni nyinyi; tukawapelekea mvua nyingi na tukaifanya mito inapita chini yao. Mwishoe tukawaangamiza kwa madhambi yao; na tukaanzisha baada yao kizazi kingine.⁶
7. Na lau tungeli kuteremshia kitabu cha karatasi, wakakigusa kwa mikono yao, wangueli sema walio kufuru: Haya si chochote ila ni uchawi dhaahiri.⁷
8. Na wao husema: Mbona hakuteremshiwa Malaika? Na kama tungeli teremsha Malaika, basi bila ya shaka ingesha hukumiwa amri, tena hapo wasingeli pewa muhula.⁸
9. Na kama tungeli mfanya Malaika bila ya shaka tungeli mfanya kama binaadamu, na tungeli watilia matatizo yale wanayo yatatiza wao.⁹
10. Na hakika Mitume walio kabla yako walifanyiwa kejeli, lakini walio wafanyia kejeli wakaja kuzungukwa na yale yale waliyo kuwa wao wanayafanyia kejeli.¹⁰
11. Sema: Tembeeni ulimwenguni, kisha mtazame ulikuwaje mwisho wa wanao

kila mmoja wenu ana zama maalumu za uhai, kisha uhai huo unakwisha kwa kufa. Na muda maalumu ulio wewka wa kufufuliwa kutoka kaburini uko kwake Yeye pekee. Kisha tena enyi makafiri! Mnabisha uwezo wa Mwenyezi Mungu kufufua, na kustahiki kwake peke yake kuabudiwa?

3 Na ni Yeye peke yake anaye stahiki kuabudiwa katika mbingu na katika ardhi. Anajua kila mnacho kificha na mnacho kionyesha. Na anajua yote mnayo yatenda, Naye atakulipeni kwa hayo.

4 Wala washirikina hawaletewi ishara yoyote katika ishara za Muumbaji wao zinazo shuhudia Umoja wake na ukweli wa Mitume wake, ila wao huikataa na kuibezwa ishara hiyo, wala hawaizingatii, wala hawaitii maanani!

5 Wao wameikanusha Qur'ani ilipo wajia, na ilhali hiyo ni Haki isiyo changanyika na upotovu! Basi yatawapata mateso ya duniani, na adhabu ya Akhera, kama ilivyo eleza Qur'ani. Na hapo utawabainikia ukweli wa onyo lake walilo kuwa wakilifanyia maskhara.

6 Hivyo wao hawajui kuwa kabla yao tuliwaangamiza umati kwa umati? Tuliwapa sababu za nguvu na kuselelea katika nchi tusizo pata kukupeni nyinyi, enyi makafiri. Na tuliwakunjulia riziki na starehe. Tukawateremshia mvua nyingi iliyo wanufaisha katika maisha yao, na tukaifanya mito inapita chini ya majumba yao ya fakhari. Nao basi wasishukuru kwa neema hizo. Kwa hivyo tukawaangamiza kwa sababu ya ushirikina wao na kukithiri dhambi zao. Baada yao tukawaleta watu wengine walio bora kuliko wao.

7 Ewe Nabii! Hata tungeli kuteremshia dalili ya ujumbe wako iliyo andikwa katika karatasi, na wao wakaiona kwa macho yao, na wakahakikisha kwa kuiweka mikono yao juu yake, basi pia wangueli sema kwa chuki tu: Hichi tunacho kigusa si chochote ila ni uchawi tu.

8 Tena wanasema: Tunataka Mwenyezi Mungu amteremshia Malaika huyu anaye dai Utume amsadikishe! Na lau kuwa Sisi tungeli waitikia hilo ombi lao, tukampeleka Malaika kama walivyo toa shauri, kisha wakafanya inda yao wasiumamini, basi amri ya kuwaangamiza ingesha pitishwa, tena hao wasinge pewa muhula hata chembe.

9 Na lau kuwa tunge jaalia huyo wa kumuunga mkono Mtume ni Malaika kama watakavyo hao, basi tungeli mfanya katika sura ya mwanaadamu, ili wapate kumwona na kufahamiana naye. Kwani wao hawawezi kumwona Malaika katika sura yake ya asili. Tena mambo yangeli watatiza na kuwadanganyikia kwa kupelekwa kwa sura ya mwanaadamu, na tungeli watia katika makosa yale yale yalio wazonga. (Tazama Maelezo 6:9)

10 Ewe Nabii! Makafiri waliwafanyia maskhara mengi Mitume wa kabla yako. Adhabu waliyo waonya nayo Mitume wao iliwazunguka hao wafanyao maskhara. Na kwanza hayo ndio waliyo kuwa wakiyakejeli.

kanusha.¹¹

12. Sema: Ni vya nani viliomo katika mbingu na katika ardhi? Sema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Yeye amejilazimisha nafsi yake kurehemu. Hakika atakukusanyeni Siku ya Kiyama isiyo kuwa na shaka. Walio jikhasiri wenyewe hawaamini.¹²

13. Na ni vyake vilio tulia usiku na mchana. Naye ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.¹³

14. Sema: Je, nimchukue rafiki mlinzi asiye kuwa Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye Muumba mbingu na ardhi, naye ndiye anaye lisha wala halishwi? Sema: Mimi nimeamrisha niwe wa kwanza wa wenye kusilimu. Na wala kabisa usiwe miongoni wa washirikina.¹⁴

15. Sema: Mimi naogopa adhabu ya Siku kubwa hiyo ikiwa nitamuasi Mola wangu Mlezi.¹⁵

16. Siku hiyo yule atakaye epushwa nayo adhabu hiyo atakuwa Mwenyezi Mungu amemrehemu. Na huko ndiko kufuzu kulio wazi.¹⁶

17. Na ikiwa Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye. Na ikiwa akikugusisha kheri, basi Yeye ndiye Mwenye uweza wa kila kitu.¹⁷

18. Naye ndiye Mwenye nguvu juu ya waja wake, na ndiye Mwenye hikima na Mwenye khabari zote.¹⁸

19. Sema: Kitu gani ushahidi wake mkubwa kabisa? Sema: Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye shahidi baina yangu na nyinyi. Na nimefunuliwa Qur'ani hii ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayo mfikia. Ati kweli nyinyi mnashuhudia kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu wapo miungu wengine? Sema: Mimi sishuhudii hayo. Sema: Hakika Yeye ni Mungu mmoja tu, nami ni mbali na mnao washirikisha.¹⁹

11 Ewe Nabii! Waambie hawa makafiri: Nendeni pande zote duniani, mzingatie vipi maangamio yalivyo kuwa mwisho wa wanao wakanusha Mitume wao. Uzingatieni vyema mwisho huu na khatima hiyo.

12 Ewe Nabii! Waambie hawa wapinzani: Nani Mmiliki mbingu na ardhi, na viliomo ndani yao? Wakiemewa, wape jawabu ambayo hakuna nyengineyo, nayo ni: Hakika Mwenye kuvimiliki vyote hivyo ni Mwenyezi Mungu peke yake, wala hana mshirika. Na Yeye amejijawabisha Mwenyewe rehema kuwarehemu waja wake. Kwa hivyo hawafanyii haraka kuwaadhibu, na anakubali toba yao. Hakika, atakukusanyeni Siku ya Kiyama ambayo haina shaka. Walio zipoteza nafsi zao, na wakazipelekea kwenye adhabu katika Siku hii, ni wale ambao hawamsadiki Mwenyezi Mungu, wala Siku ya Hisabu.

13 Ni vya Mwenyezi Mungu vya kila zama, kama ilivyo kuwa vyake vya kila pahala. Naye ndiye Mwenye kusikia kila la kusikiwa, na Mwenye kujua kila la kujulikana.

14 Sema ewe Nabii! Mimi simfanyi yeyote kuwa ni mungu na msaidizi isipo kuwa Mwenyezi Mungu, Allah, tu. Yeye peke yake ndiye aliye ziumba tangu mwanzo mbingu na ardhi kwa nidhamu isiyo kuwa na kiigizo kilicho tangulia. Naye ndiye Mwenye kuwaruzuku chakula waja wake, wala Yeye hahitaji kwao chakula. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu ameniamrisha niwe wa mwanzo wa kusilimu, na amenikataza kumshirikisha Yeye na yeyote mwinginewe katika kumuabudu.

15 Sema: Mimi naogopa, nikenda kinyume na amri ya Mola Mlezi wangu na nikamuasi nisije nikapata adhabu ya hiyo Siku ya shida.

16 Mwenye kuepushwa adhabu hii Siku ya Kiyama, basi Mwenyezi Mungu amemrehemu. Na huko ndiko kufuzu kulio thibiti, kulio wazi.

17 Mwenyezi Mungu akikupatiliza kwa ovu, basi hapana wa kuliondoa hilo ila Yeye Mwenyewe. Na akikupa kheri basi hapana awezae kuirudisha fadhila yake, kwani Yeye ni Muweza wa kila kitu.

18 Yeye ndiye Mwenye kushinda kwa uwezo wake, Aliye juu, juu ya waja wake, Aliye sifika kwa hikima katika kila alifanyalo, Mwenye kuvizunguka kwa ujuzi wake vinavyo onekana na vinavyo fichikana.

19 Ewe Nabii! Waambie hao wanao kukanusha na wanao taka ushahidi wa Utume wako: Kitu gani chenye ushahidi mkubwa, na chenye kustahiki kusadikiwa kuliko vyote? Kisha uwambie: Hakika Mwenyezi

20. Wale Tulio wapa Kitabu wanayajua haya kama wanavyo wajua watoto wao. Wale walio zikhasiri nafsi zao hawaamini.²⁰
21. Na nani dhaalimu zaidi kuliko anaye mzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na akazikanusha Ishara zake? Hakika madhaalimu hawafanikiwi.²¹
22. Siku tutapo wakusanya wote pamoja, kisha tuwaambie walio shirikisha: Wako wapi washirikishwa wenu mlio kuwa mnadai?²²
23. Kisha hautakuwa udhuru wao ila ni kusema: Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.²³
24. Tazama jinsi wanavyo jisemea uwongo wenyewe. Na yamewapotea waliyo kuwa wakiyazua.²⁴
25. Na wapo miongoni mwao wanao kusikiliza; na tumezitia pazia nyoyo zao wasije kuyafahamu. Na upo uziwi masikioni mwao, na wakiona kila Ishara hawaiamini. Hata wakikujia kwa kujadiliana nawe, wanasema walio kufuru: Hizi si chochote ila hadithi za watu wa kale.²⁵
26. Nao huwazuia watu, na wao wenyewe wanajitenga nayo. Nao hawaangamizi ila nafsi zao tu, wala wao hawatambui.²⁶
27. Na unge ona watakapo simamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti

Mungu ndiye shahidi mkubwa kushinda wote wa kushuhudia baina yangu na nyinyi katika ukweli wa haya ninayo kuleteeni. Na Yeye ndiye aliye iteremsha hii Qur'ani ili iwe ni hoja ya ukweli wangu, nipate kukuhadharisheni nyinyi na kila itakayo mfikia khabari yake. Nayo ni hoja ya kukata, inayo shuhudia ukweli wangu. Kwani nyinyi hamwezi kuleta mfano wake! Waulize: Hivyo nyinyi mnaitakidi kuwa Mwenyezi Mungu ana miungu wenziwe? Kisha uwambie: Mimi sishuhudii hayo, wala sisemi hivyo, wala sikukubaliani kwa hayo. Hapana shaka wa kuabudiwa kwa haki ni Mungu Mmoja. Na mimi ni mbali kabisa na hayo masanamu mnayo mshirikisha Naye.

20 Tulio wapa Vitabu vya mbinguni, Mayahudi na Wakristo, wanamjua vyema Muhammad na ukweli wa Utume wake kutokana na hivyo Vitabu vyao vya Biblia, kama wanavyo wajua watoto wao. Walio zipoteza nafsi zao hawayakubali yale wanayo yajua. Kwa hivyo hao hawaamini.

21 Na hapana mtu aliye zidi kuidhulumu nafsi yake na Haki, kuliko anaye mzulia Mwenyezi Mungu uwongo, na akadai kuwa Yeye *Subhanahu* ana mwana au mshirika, au akamwambatisha lolote lisilo laiki yake, au akazikanya dalili zenye kuonyesha Umoja wake Mwenyezi Mungu na ukweli wa Mitume wake. Hakika madhaalimu hawatopata kheri duniani wala Akhera.

22 Na watajie yatakayo tokea Siku tutapo kusanya viumbe vyote kwa ajili ya hisabu. Kisha tutawaambia kwa kuwahizi walio kuwa wakiwaabudu wenginewe pamoja na Mwenyezi Mungu: Wako wapi mlio wafanya ni washirika wa Mwenyezi Mungu, wapate kukufaeni?

23 Kisha hayatakuwa matokeo ya hayo matatizo yao magumu pahala hapo ila kujitoa kimaso-maso kutokana na ushirikina wao kwa kusema uwongo. Waseme: Wallahi Mola Mlezi wetu! Hatukumshirikisha nawe yeyote katika ibada.

24 Angalia vipi wanavyo jitia makosani wenyewe kwa uwongo huu. Na vile walivyo kuwa wameviunda wenyewe kwa kuviabudu, navyo ni mawe tu, na wakadai kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu, sasa vimewapotea.

25 Na miongoni mwao wapo wanao kusikiliza unapo soma Qur'ani, si kwa sababu waifahamu na ipate kuwaongoa, lakini ni kwa ajili wapate njia ya kuitoa komba na kuikejeli.

Na Sisi kwa sababu hiyo tumewazuilia wasiweze kunafika kwa akili zao na masikio yao. Imekuwa kama kwamba akili zao zimefunikwa haziwezi kuelewa baraabara; na kama kwamba masikio yao yana uziwi unao wazuia wasizisikie Aya za Qur'ani. Na hawa hata wakiona kila dalili hawaamini. Hata wakikujia wakujadili kwa upotovu wanasema walio kufuru, huku wakisukumiza na ukafiri wao: Haya si chochote ila hadithi za uwongo zilizo tungwa na watu wa zamani wa kabla yako.

26 Wao huwazuia watu wasihamini Qur'ani, na wao wenyewe hujitenga nayo. Inakuwa wao hawanafiki, wala hawawachii wenginewe wakanafika! Na kwa kitendo hicho hawadhuru ila nafsi zao, na wao hawatambui ubaya wa wayatendayo.

tungeli rudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni wa Waumini.²⁷

28. Bali yamewadhihirikia waliyo kuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangeli rudishwa bila ya shaka wange yarejea yale yale waliyo katazwa. Na hakika hao ni waongo.²⁸

29. Na walisema: Hakuna mengine ila maisha yetu haya ya duniani, wala sisi hatutafufuliwa.²⁹

30. Na lau ungesi ona watavyo simamishwa mbele ya Mola wao Mlezi, akawaambia: Je, si kweli haya? Na wao watasema: Kwani? Tunaapa kwa Mola Mlezi wetu ni kweli. Yeye atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya vile mlivyo kuwa mnakataa.³⁰

31. Hakika wamekhasirika walio kanusha kukutana na Mwenyezi Mungu, mpaka ilipo wajia Saa kwa ghafla, wakasema: Ole wetu kwa tuliyo yapuuzi! Nao watabeba mizigo yao juu ya migongo yao. Ni maovu hayo wanayo yabeba.³¹

32. Na maisha ya dunia si chochte ila ni mchezo na pumbao tu. Na hakika nyumba ya Akhera ni bora zaidi kwa wanao mcha Mungu. Basi, je, hamtii akilini?³²

33. Tunajua ya kwamba yanakuhuzunisha wanayo yasema. Basi hakika wao hawakukanushi wewe, lakini hao madhaalimu wanazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu.³³

34. Na hakika walikanushwa Mitume wa kabla yako. Nao wakavumilia kule

27 Ewe Nabii! Lau ungesi waona hawa makafiri, watavyo simama mbele ya Moto wakisononeka na vitisho vyake, ungesi ona jambo la ajabu lenye kutisha, nao wanatamani warejeshwe tena duniani, wakisema: Laiti tungeli rudishwa duniani tukatengeneza tuliyo yaharibu! Wala hatutakanusha Ishara za Mola wetu Mlezi. Na tutakuwa miongoni wa Waumini.

28 Na kauli yao hii haikuwa ila kwa kuwa haimkiniki tena kuficha wala kufanya ukaidi katika yale anayo waambia Mtume. Na lau kama wakirudishwa duniani wataurejea tena ukafiri alio wakataza Mwenyezi Mungu. Haya ni kwa ghururi zao kughurika na mapambo ya dunia, na kwa kufuata kwao matamano yao. Na hakika hao wanasema uwongo kwa kudai kuwa wataamini pindi wakirejeshwa duniani.

29 Na lau wakirejeshwa duniani watairudia ile ile sera yao ya mwanzo, na watasema: Hatuna sisi uhai mwingine ila huu uhai wa kidunia. Wala sisi hatutafufuliwa baadae.

30 Lau ungesi waona watavyo simama mbele ya Mola wao Mlezi kwa ajili ya kuhisabiwa, na wao wanaujua ukweli wa aliyowateremshia Mwenyezi Mungu Mitume wake, ungesi ona uovu wa hali yao pale Mwenyezi Mungu atapo waambia: Je, haya mnayo yashuhudia sasa sio kweli mliyo kuwa mkiikataa huko duniani kwenu? Nao watajibu hali ni wanyonge: Kwani! Tunaapa kwa Mola Mlezi wetu, ni kweli! Tena baada ya hayo Mwenyezi Mungu atawaambia: Ingieni Motoni kwa sababu ya mlivyo kuwa mmeshikilia ukafiri.

31 Hakika wamekhasiri walio kanya kukutana na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya hisabu na malipo ya Siku ya Kiyama, na wakaendelea na kukanusha kwao mpaka yalipo wafuma mambo ya Siku ya Kiyama wakajuta na wakasema: Ole wetu (yaani msiba wetu) kwa kupuuzi kwetu kuifuata Haki huko duniani! Nao siku hiyo watakuwa wanaanguka kwa kuemewa na uzito wa dhambi zao! Ni mabaya mno hayo madhambi wanayo yabeba.

32 Na huo uhai wa duniani walio uona makafiri kuwa ndio uhai wa pekee, na ambao hawaukusudii kwa kufanya vitendo vya kumridhi Mwenyezi Mungu, uhai huo si chochote ila ni mchezo usio kuwa na manufaa, na pumbao la kujipumbazia tu!! Na hakika nyumba ya Akhera ndio khasa uhai wa kweli. Huo unawanufaisha zaidi wale wanao mwogopa Mwenyezi Mungu na wanazifuata amri zake. Basi hamtii akilini jambo hili lililo wazi? Hivyo hamfahamu linalo kudhuruni na linalo kufaeni?

33 Ewe Nabii! Sisi tunajua kuwa yanakuhuzunisha haya wayasemayo makafiri ili kukukadhibisha. Basi wewe usihuzunike kwa hayo. Kwani hakika wao hawakutuhumu wewe kuwa ni mwongo, walakini wao kwa kujidhulumu nafsi zao na kuidhulumu haki, wanashindana kwa inda, na wanazikanya kwa ndimi zao dalili za ukweli wako, na alama za Unabii wako.

kukanushwa, na kuudhiwa, mpaka ilipo wafikia nusura yetu. Na hapana wa kubadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu. Na bila ya shaka zimekuja baadhi ya khabari za Mitume hao.³⁴

35. Na ikiwa ni makubwa kwako huku kukataa kwao, basi kama unaweza kutafuta njia ya chini kwa chini ya ardhi, au ngazi kwendea mbinguni ili uwalettee Ishara -- Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angependa angeli wakusanya kwenye uwongofu. Basi usiwe miongoni mwa wasio jua.³⁵

36. Hakika wanao kubali ni wale wanao sikia. Na ama wafu Mwenyezi Mungu atawafufua, na kisha kwake Yeye ndio watarejeshwa.³⁶

37. Na wamesema: Kwa nini hakuteremshiwa muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Sema: Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuteremsha muujiza. Lakini wengi wao hawajui.³⁷

38. Na hapana mnyama katika ardhi, wala ndege anaye ruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi. Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa.³⁸

39. Na walio kanusha Ishara zetu ni viziwi na mabubu waliomo gizani. Mwenyezi Mungu humwachia kupotea amtakaye, na humweka katika Njia iliyo nyooka amtakaye.³⁹

34 Na hakika Mitume wa kabla yako walikabiliwa na ukanushi na maudhi kutokana na kaumu zao, kama walivyo kufanyia wewe kaumu yako. Nao wakasubiri juu ya kukanushwa na kuudhiwa, mpaka tulipo wanusuru. Basi nawe subiri kama walivyo subiri wao, mpaka ikujie nusura yetu. Wala hapana la kugeza ahadi ya Mwenyezi Mungu kuwa atawanusuru wenye kusubiri. Lazima hayo yatimie. Na Sisi tumekusimulia kutokana na khabari za hao Mitume, na tulivyo waunga mkono. Ndani ya hayo mna maliwaza yako, na maelezo kuwa yeyote mwenye kuchukua Ujumbe lazima ahimili kila namna ya shida.

35 Ikiwa unaona dhiki kwa kukataa kwao kuitikia wito wako, basi kama unaweza kutafuta njia ya kupita chini ya ardhi, au ngazi ya kupandia mbinguni ukawaletea dalili ya kuthibitisha ukweli wako, fanya hivyo! Lakini huna uwezo huo. Basi poa roho yako, na usubiri kungojea hukumu ya Mola Mlezi wako. Lau kuwa Mwenyezi Mungu ange penda basi angeli walazimisha wote hao wayaamini ulio kuja nayo, wakitaka wasitake. Lakini Yeye amewaacha kwa ajili ya kuwafanyia mtihani, kuwajaribu. Basi usiwe miongoni mwa wasio ijua hukumu ya Mwenyezi Mungu na mwendo wake kwa viumbe.

36 Hakika wanao itikia wito wa Haki ni wale wanao ukubali - wale ambao wanao sikia kwa msikio wa kufahamu na kuzingatia. Ama hao walio potoka kabisa hawanafiiki kwa wito wako, kwani wao wamo katika hukumu ya maiti. Na Mwenyezi Mungu atawafufua kutoka makaburini Siku ya Kiyama, na atawarejeza kwake awahisabu kwa waliyo yafanya.

37 Na makafiri washupavu wamesema: Tunataka atermshiwe Muhammad dalili ya kuonekana kutoka kwa Mola wake Mlezi, itayo shuhudia ukweli wa huu wito wake! Waambie, ewe Nabii: Hakika Mwenyezi Mungu anaweza kuteremsha hiyo dalili muitakayo. Lakini wengi wao hawajui nini hikima ya Mwenyezi Mungu katika kuziteremsha Ishara. Na hayo hayafuati matamano yao. Na lau kuwa Yeye akiwakubalia hilo walitakalo, na kisha wakakanusha baada yake, basi atawateketeza tu. Lakini wengi wao hawajui nini matokeo ya vitendo vyao!!

38 Na dalili yenye nguvu kabisa ya uwezo wa Mwenyezi Mungu na hikima yake, na rehema yake, ni kuwa Yeye kaumba kila kitu, na wala hapana juu ya ardhi mnyama anaye tambaa juu yake au chini yake, wala ndege arukaye kwa mbawa zake katika anga, ila Mwenyezi Mungu amewaumba kuwa ni jamii za umati kama mlivyo nyinyi. Na amewajaalia wawe na sifa zao, na vitambulisho vyao, na mipango yao ya maisha yao. Hatukukiacha kitu katika Kitabu kilicho andikwa kilioko kwetu ila tumekithibitisha. Na ikiwa wanakanusha, basi watafufuliwa pamoja na kaumu zote kwa ajili ya hisabu Siku ya Kiyama.

39 Na ambao hawakuzisadiki dalili zetu zinazo onyesha uwezo wetu na ukweli wa Utume wako, basi hao hawakunafiika na hisiya zao kuwawezesha kuitambua Haki. Kwa hivyo wakawa wanababaika katika upotovu wa ushirikina na inda, kama anavyo babaika kiziwi-bubu katika giza la usiku, hawezi kuepuka kuangamia. Lau kuwa watu hawa wameelekea kheri Mwenyezi Mungu angeli wawezesha wamfikie,

40. Sema: Mwaonaje ikikujieni adhabu ya Mwenyezi Mungu, au ikakufikieni hiyo Saa - mtamwomba asiye kuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi ni wakweli?⁴⁰
41. Bali Yeye ndiye mtakaye mwomba, naye atakuondoleeni mnacho mwombea akipenda. Na mtasahau hao mnao wafanya washirika wake.⁴¹
42. Na kwa yakini tulipeleka Mitume kwa kaumu zilizo kuwa kabla yako, kisha tukazitia katika dhiki na mashaka ili zipate kunyenyekea.⁴²
43. Kwa nini wasinyenyekee ilipo wafika adhabu yetu? Lakini nyoyo zao zilikuwa ngumu, na Shet'ani akawapambia waliyo kuwa wakiyafanya.⁴³
44. Basi walipo saha walio kumbushwa tuliwafungulia milango ya kila kitu. Mpaka walipo furahia yale waliyo pewa tuliwashika kwa ghafla, na mara wakawa wenye kukata tamaa.⁴⁴
45. Ikakatwa mizizi ya watu walio dhulumu - na wa kuhimidiwa ni Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.⁴⁵
46. Sema: Mwaonaje Mwenyezi Mungu akanyakua kusikia kwenu, na kuona kwenu, na akaziziba nyoyo zenu, ni mungu gani asiye kuwa Mwenyezi Mungu ataye kuleteeni hayo tena? Angalia vipi tunavyo zieleza Ishara, kisha wao wanapuuza.⁴⁶
47. Sema: Mwaonaje, ikikufikieni adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa ghafla, au kwa dhaahiri, jee wataangamizwa isipo kuwa walio dhulumu?⁴⁷

kwani Yeye *Subhanahu* akitaka kumpoteza mtu kwa ufisadi wake alio ukusudia, basi humwachilia mbali na shani yake; na akitaka kumwongoa mtu kwa kuwa makusudio yake ni sawa, basi humsahilishia njia ya Imani iliyo wazi na iliyo nyooka.

40 Ewe Nabii! Waambie hawa makafiri: Nambieni, ikikujieni adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu hapa duniani, au ikikujieni Kiyama kwa vitisho vyake, mtamuelekea yeyote asiye kuwa Mwenyezi Mungu mkimnyenyekea wakati huo akufaeni kwa lolote, kama nyinyi mnasema kweli katika kumuabudu kwenu asiye kuwa Mwenyezi Mungu?

41 Bali nyinyi mnamuelekea Yeye mnapo muomba akakuondoleeni mnacho taka kiondolewe, pindi akipenda. Na mnapo kuwa katika hali hii ya shida mnawasahau hao mnao wafanya ni washirika wake Mwenyezi Mungu!!

42 Yasikudhiki, ewe Nabii, yanao kupata kwa watu wako. Kwani Sisi tuliwapeleka Mitume kabla yako kwa kaumu nyingi kabla ya umma wako huu, nao wakawaambia ni waongo. Nasi tukawapatiliza kwa adhabu zilizo wateremkia, na yaliyo wadhuru miili yao, ili walau wanyenyekee na warejee kwa Mwenyezi Mungu.

43 Na lililo takikana ni kuwa warejee kwa Mola wao Mlezi. Lakini hawakufanya hayo. Bali zikaendelea nyoyo zao katika ugumu wao, na Shetani akawapambia vile vitendo vyao vibaya, (wakaviona vizuri).

44 Walipo acha kuwaidhika kwa ufakiri na maradhi tulio wapa kuwa ni mtihani, tukawajaribu baada yake kwa kuwapa riziki zenye wasaa. Tukawafungulia milango ya kila sababu za riziki, mpaka walipo furahia neema zetu, na wao wasimshukuru Mwenyezi Mungu kwa hayo, ikawajia adhabu ghafla. Wakawa wanadahadari, wamekata tamaa, hawaipati njia ya kuokoka.

45 Ikateketezwa kabisa kaumu hii, yenye kudhulumu, asibakie hata mmoja. Alhamdulillah, wa kuhimidiwa kwa sifa zote njema ni Mwenyezi Mungu, mwenye kuwalea viumbe kwa neema na nakama, na mwenye kuisafisha ardhi na ufisadi wa wenye kudhulumu.

46 Waambie, ewe Nabii: Hebu nambieni--Mwenyezi Mungu akinyakua kusikia kwenu, na akazifunika nyoyo zenu zisiweze kutambua kitu, akakufanyeni viziwi, vipofu hamfahamu kitu - mtamuabudu mungu gani isipo kuwa Mwenyezi Mungu atakae weza kukurejesheni aliyo kunyang'anyeni Mwenyezi Mungu? Ewe Nabii! Tazama vipi tunavyo ziweka wazi hoja na kuzipanga mbali mbali. Kisha pamoja na haya wao wanakataa kuzizingatia na kunafiika kwazo.

47 Sema: Hebu nambieni--Ikikufikieni adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa ghafla bila ya kuitarajia, au ikakujieni kwa dhaahiri nanyi mnaitaraji, kwa kuwa mmeonywa kuwa itakuja - hivyo adhabu hiyo itamsibu yeyote ila wale watu walio jidhulumu nafsi zao kwa kushikilia ukafiri na upotovu? Hakika

- 48.** Na hatuwatumi Mitume ila huwa ni wabashiri na waonyaji. Na wenye kuamini na wakatenda mema haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.⁴⁸
- 49.** Na walio kanusha Ishara zetu itawagusa adhabu kwa walivyo kuwa wakipotoka.⁴⁹
- 50.** Sema: Mimi sikwambiini kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu. Wala sijui mambo yaliyo fichikana. Wala sikwambiini kuwa mimi ni Malaika. Mimi sifuati ila yanayo funuliwa kwangu. Sema: Je, wanakuwa sawa, kipofu na mwenye kuona. Basi hamfikiri?⁵⁰
- 51.** Na waonye kwayo wanao ogopa kuwa watakusanywa kwa Mola wao Mlezi, hali kuwa hawana mlinzi wala mwombezi isipo kuwa Yeye, ili wapate kuchamngu.⁵¹
- 52.** Wala usiwafukuze wanao mwomba Mola Mlezi wao asubuhi na jioni kwa kutaka radhi yake. Si juu yako hisabu yao hata kidogo, wala hisabu yako si juu yao hata kidogo, hata uwafukuze na uwe miongoni mwa wenye kudhulumu.⁵²
- 53.** Na hivi ndivyo tunavyo wajaribu wao kwa wao, ili waseme: Ni hao ndio Mwenyezi Mungu amewafadhilisha miongoni mwetu? Kwani Mwenyezi Mungu hawajui wanao shukuru?⁵³
- 54.** Na wanapo kujia wanao ziamini Ishara zetu waambie: Assalamu alaikum! Amani iwe juu yenu! Mola wenu Mlezi amejilazimisha rehema, ya kwamba atakaye fanya uovu miongoni mwenu kwa ujinga, kisha akatubu baada yake na akatengenea, basi hakika Yeye ni Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu.⁵⁴

haitamsibu mwenginewe.

48 Na Sisi hatuwatumi Manabii ila ni kwa ajili ya kuwabashiria wenye kuamini mambo ya kheri na thawabu, na kuwahadharisha na adhabu wale wanao kufuru. Basi wenye kuuamini wito wao, na wakatenda mema, hawatakuwa na khofu ya kuwapata shari, wala hawatahuzunika kwa kuikosa kheri.

49 Na wale wanao zikanusha dalili zilizo wazi za ukweli wa waliyo kuja nayo Mitume, watapata adhabu kwa kutoka kwao kwenye ut'iifu na Imani.

50 Ewe Mtume! Waambie hawa makafiri: Mimi sikwambiini kuwa mimi nina madaraka aliyo nayo Mwenyezi Mungu hata nikuitikieni kwa mnayo yataka. Wala sidai kuwa mimi nina ilimu ya mambo ya ghaibu, ambayo Mwenyezi Mungu hakunijuvya. Wala sisemi kuwa mimi ni Malaika ninaweza kupanda mbinguni! Mimi si chochote ila ni mwanaadamu tu. Sifuati ila Mwenyezi Mungu anacho nifunulia. Sema ewe Nabii: Je, wanakuwa sawa, aliye potoka na aliye ongoka katika kuzijua kweli hizi? Hivyo, inakuelekeeni nyinyi mkautupa uwongofu ninao kuleteeni, msiuzingatie kwa akili zenu hata ikakubainikieni Haki?

51 Na wahadharishe kwa yaliyomo katika hii Qur'ani wale wanayo khofu vitisho vya Siku watapo wachunga Malaika kwa ajili ya hisabu na malipo, Siku ambayo itayo kuwa haina wa kunusuru wala kuombea ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, wahadharishe wajitenge mbali na vinavyo mkasirisha Mwenyezi Mungu.

52 Na ewe Nabii! Usiitikie wito wa makafiri walio panda vichwa, ukawatenga Waumini wanyonge, wanao muabudu Mwenyezi Mungu daima, wala hawatafuti ila radhi zake. Wala usivishughulikie vitimbi vya washirikina juu ya hawa Waumini. Kwani wewe mbele ya Mwenyezi Mungu huna jukumu juu ya vitendo vyao, kama wao wasivyo kuwa na jukumu juu ya chochote katika vitendo vyako. Na ukiwakubalia hawa makafiri wenye kani, na ukawatenga Waumini, utakuwa miongoni mwa walio dhulumu.

53 Na kwa majaribu kama haya ambayo ndio ada yetu kuyatenda, tukawafanyia mtihani walio takabari kwa kuwatanguliza wanyonge wawe mbele kusilimu; wapate kusema wenye kiburi, wanao pinga, wakifanya kejeli: Hivyo ni hawa mafakiri ndio alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwetu sote kwa kuwapa hiyo kheri aliyo waahidi Muhammad? Hakika hawa mafakiri wanaijua neema ya Mwenyezi Mungu juu yao kwa kuwapa tawfiki ya kuifikia Imani, na kwa hivyo wanamshukuru. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua zaidi nani anashukuru fadhila yake na neema yake.

54 Na wakikujia wanao isadiki Qur'ani waambie kwa kuwahishimu: Assalamu Alaikum, Amani juu yenu. Nakubashirieni rehema kunjufu ya Mwenyezi Mungu, ambayo amejilazimisha Yeye Mwenyewe, kwa fadhila yake, na ambayo inahukumu kuwa yeyote katika nyinyi akitenda ubaya bila ya kuzingatia

55. Na ndio hivi tunavyo zieleza Ishara ili ibainike njia ya wakosefu.⁵⁵
56. Sema: Mimi nimekatazwa kuwaabudu hao mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu. Sema: mimi sifuati matamano yenu. Hivyo nitakuwa nimepotea, na sitakuwa miongoni mwa walio ongoka.⁵⁶
57. Sema: Mimi nipo kwenye sharia iliyo wazi itokayo kwa Mola wangu Mlezi, nanyi mnaikanusha. Mimi sinacho hicho mnacho kihimiza. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu. Yeye anasimulia yaliyo kweli; naye ni Mbora wa kuhukumu kuliko wote.⁵⁷
58. Sema: Lau kuwa ninacho hicho mnacho kihimiza, ingeli kwisha katwa shauri baina yangu na nyinyi. Na Mwenyezi Mungu anawashinda wote kuwajua madhaalimu.⁵⁸
59. Na ziko kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinacho bainisha.⁵⁹
60. Naye ndiye anaye kufisheni usiku, na anakijua mlichio fanya mchana. Kisha Yeye hukufufueni humo mchana ili muda ulio wekwa utimizwe. Kisha kwake Yeye ndiye marejeo yenu, na tena akwambieni mliyo kuwa mkiyafanya.⁶⁰
61. Naye ndiye Mwenye nguvu za kushinda, aliye juu ya waja wake. Na hukupelekeeni waangalizi, mpaka mmoja wenu yakimjia mauti wajumbe wetu humfisha, nao hawafanyi taksiri.⁶¹
62. Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki. Hakika, hukumu

matokeo yake, kisha akarejea kwa Mwenyezi Mungu naye amejuta, ametubu, na akatengeneza a'mali zake, basi Mwenyezi Mungu atamghufiria, kwani Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghfira, na mkunjufu wa rehema.

55 Na kwa mfano wa bayana hiyo iliyo wazi, tunaweka wazi dalili mbali mbali, ipate kudhihiri njia ya Haki wanayo ipitia Waumini, na ibainishe njia ya upotovu wanayo ipitia makafiri.

56 Ewe Nabii! Waambie hawa makafiri: Hakika Mwenyezi Mungu amenikataza kuwaabudu hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Basi mimi sifuati matamano yenu. Kwani nikikufuateni nitakuwa nimekengeuka kuiacha Haki, na sitokuwa katika waongofu!

57 Waambie: Mimi nipo juu ya Sharia iliyo wazi, iliyo teremshwa kutoka kwa Mola wangu Mlezi. Na nyinyi mmeikanusha Qur'ani iliyo ileta Sharia hii. Na mimi sina uwezo kuileta hiyo adhabu mnayo ihimiza ije. Bali hayo yamo katika uwezo wa Mwenyezi Mungu, na yamelazimika na kupenda kwake na hikima yake. Na hakuna amri wala madaraka ila ya Mwenyezi Mungu tu. Akipenda Yeye atakuleteeni adhabu kwa haraka, na akipenda ataichelewesha. Yeye *Subhanahu*, Aliye takasika, anafuata katika hayo hikima yake, naye ni mbora wa kuhukumu baina yangu na nyinyi.

58 Sema: Lau ingeli kuwa kumo katika makadara yangu kukuteremshieni hiyo adhabu mnayo ihimiza ije, ningeli kuteremshieni kwa kukasirika kwa ajili ya Mola Mlezi wangu. Na hapo mambo yangeli kwisha baina yangu na nyinyi. Walakini amri ni ya Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mwenye kujua kuliko wote wanayo stahiki makafiri katika adhabu ya haraka, au ya kuakhirika.

59 Ni Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye ujuzi wa milango yote ya vilio ghaibu, visio juulikana na wengine. Hapana Mwenye kukusanya ujuzi wa hivyo ila Yeye, na anao wataka kuwapa baadhi yake. Naye ujuzi wake umekusanya vitu vyote vilioko nchi kavu na vilioko baharini. Wala halidondoki jani, jani lolote lile, ila Yeye analijua, wala haianguki mbegu chini ya ardhi, wala chochote kilicho kinyevu au kikavu, ila Yeye *Subhanahu* anakijua kwa utimilifu. (*Tazama* Maelezo 6:59)

60 Na Yeye ndiye anakulazeni usiku, na anakuamsheni mchana. Na anajua mnayo yachuma, mpaka utimie muda wa kumfikia kila mmoja wenu ajali yake duniani ya kufa. Kisha Siku ya Kiyama mtarejeshwa nyote nyinyi kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Tena atakwambieni a'mali zenu mlizo tenda duniani, njema au mbaya, na akulipeni kwazo.

61 Naye ndiye Mwenye kushinda kwa uwezo wake, aliye tukuka kwa ufalme wake juu ya waja wake, na anaye kupelekeeni Malaika wa kudhibiti kila vitendo vyenu, mpaka ufike mwisho wa kila mmoja wenu, ishikwe roho yake na Malaika wetu tunao wapeleka kwa kazi hiyo. Na wao hao Malaika hawafanyi taksiri katika kazi walio wakilishwa kuitenda.

ni yake. Naye ni Mwepesi kuliko wote wanao hisabu.⁶²

63. Sema: Ni nani anaye kuokoeni katika giza la nchi kavu na baharini? Mnamwomba kwa unyenyekevu na kwa siri, mkisema: Kama akituokoa na haya bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wanao shukuru.⁶³

64. Sema: Mwenyezi Mungu hukuokoeni kutoka hayo, na kutoka kila mashaka, na kisha nyinyi mnamshirikisha!⁶⁴

65. Sema: Yeye ndiye Muweza wa kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu, au kukuleteeni fujo la mfarakano, na kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzao. Tazama vipi tunavyo zieleza Aya ili wapate kufahamu.⁶⁵

66. Na watu wako wameikanusha, nayo ni Haki. Sema: Mimi sikuwakilishwa juu yenu.⁶⁶

67. Kila khabari ina kipindi chake. Nanyi mtakuja jua.⁶⁷

68. Na unapo waona wanao ziingilia Aya zetu, basi jitenge nao mpaka waingilie mazungumzo mengine. Na kama Shet'ani akikusahaulisha, basi baada ya kutanabahi usikae pamoja na watu madhaalimu.⁶⁸

69. Wala wamchao Mungu hawana jukumu lolote kwao, lakini ni kukumbusha, asaa wapate kujiepusha.⁶⁹

70. Waachilie mbali walio ifanya dini yao ni mchezo na pumbao, na uhai wa dunia ukawaghuri. Nawe kumbusha kwayo, isije nafsi ikaangamizwa kwa sababu ya iliyo yachuma, nayo haina mlinzi wala mwombezi ila Mwenyezi Mungu. Na ingatoa kila fidia haitokubaliwa. Hao ndio walio angamizwa kwa sababu ya yale waliyo yachuma. Wao watapata kinywaji cha maji ya moto kabisa, na adhabu chungu. Kwa sababu ya

62 Tena hawa maiti watafufuliwa Siku ya Kiyama, na watasimamishwa mbele ya Mola Mlezi wao ambaye ndiye anayatawala mambo yao peke yake. Jueni kuwa Yeye tu ndiye wa kuamua baina ya viumbe na kuwahisabu katika Siku hiyo, naye ni Mwepesi wa kuhisabu na kulipa.

63 Ewe Nabii! Waambie washirikina: Nani anaye kuvueni na vitisho vya bara na baharini vinapo kutokeeni, mkamuaungukia na mkamwomba kwa unyenyekevu wa dhaahiri na wa ndani, mkisema: Tunaapa! Kama ukituvua na vitisho hivi tutakuwa katika wanao kiri fadhila yako, na wanao dumu kukushukuru?

64 Sema: Ni Allah, Mwenyezi Mungu wa pekee, ndiye aliye kuokoeni na vitisho hivi, na kila shida nyengineyo. Na kisha nyinyi pamoja na hayo mnamshirikisha na wengine katika ibada, ambao hawawezi kuondoa shari wala kuleta kheri!

65 Sema: Hakika ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye awezaye kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu au chini yenu, au kukufanyeni nyinyi kwa nyinyi mkawa maadui, mkawa mataifa yenye kuwa mbali mbali matamanio yao, yenye kuchukiana, mkitesana nyinyi kwa nyinyi kwa mateso machungu na makali! Angalia vipi hoja zinavyo onyesha uwezo wetu na kustahiki kwetu peke yetu kuabudiwa, ili wapate kuzingatia na kuifahamu Haki.

66 Na kaumu yako wameikanusha Qur'ani, nayo ni Haki ambayo haina cha kukanushwa ndani yake. Ewe Nabii! Waambie: Mimi sikuwekwa kuwa ni muwakilishi wa kukulindeni, na kupima vitendo vyenu na kukulipeni kwayo. Bali mambo yenu katika hayo yako kwa Mwenyezi Mungu.

67 Kila khabari iliyo letwa na Qur'ani ina wakati wake wa kutimia. Nanyi mtakuja jua ukweli wa khabari hizi zitapo tokea.

68 Na ukihudhuria katika baraza za makafiri, ukawakuta wanazikosoa Aya za Qur'ani, au wanazifanyia maskhara, basi wewe waepuke mpaka watapo ingia katika mazungumzo mengine. Na ukisahau na ukakaa nao wakati wa mazungumzo yao hayo mapotovu, kisha ukaikumbuka amri ya Mwenyezi Mungu ya kujitenga nao, basi usikae tena na watu madhaalimu baada ya kukumbuka.

69 Na wenye kumcha Mwenyezi Mungu hawana dhambi katika dhambi za hawa madhaalimu, ikiwa wataendelea na upotovu wao. Lakini yapasa kuwasemeza na kuwakumbusha, asaa huenda wakaiogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu, na wakaacha upotovu.

kukanusha.⁷⁰

71. Sema: Je, tumuombe asiye kuwa Mwenyezi Mungu ambae hatufai wala hatudhuru, na turejee nyuma baada ya Mwenyezi Mungu kwisha tuhidi? Tuwe kama ambao mashet'ani wamempumbaza katika ardhi, amebabaika? Anao marafiki wanao mwita ende kwenye uwongofu, wakimwambia: Njoo kwetu! Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio Uwongofu. Nasi tumeamrisha tusilimu kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote,⁷¹

72. Na mshike Sala, na mcheni Yeye, na kwake Yeye ndiko mtako kusanywa.⁷²

73. Naye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi kwa Haki. Na anaposema: Kuwa! Basi huwa. Kauli yake ni Haki. Na ufalme wote ni wake Siku litapo pulizwa barugumu, Mjuzi wa yaliyo fichikana na yanayo onekana. Naye ndiye Mwenye hikima na Mwenye khabari.⁷³

74. Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake, Azar: Unayafanya masanamu kuwa ni miungu? Hakika mimi nakuona wewe na watu wako mmo katika opotofu ulio wazi.⁷⁴

75. Na kadhaalika tulimwonyesha Ibrahim ufalme wa mbingu na ardhi, na ili awe miongoni mwa wenye yakini.⁷⁵

76. Na ulipo muingilia usiku akiona nyota, akasema: Huyu ni Mola Mlezi wangu. Ilipo tua akasema: Siwapendi wanao tua.⁷⁶

70 Na ewe Nabii, waachilie mbali wale walio fanya sharia yao, mwendo wao, pumbao na mchezo, na wakakhadaika na maisha ya dunia wakaacha ya Akhera. Na daima kumbusha kwa Qur'ani, na wahadharishe vitisho vya Siku ambayo nafsi itafungika na a'mali yake, itapo kuwa hapana wa kunusuru wala wa kusaidia isipo kuwa Mwenyezi Mungu. Na kila fidia ya kujiokoa haitokubaliwa. Hao makafiri watafungwa katika adhabu kwa sababu ya shari waliyo itenda. Katika Jahannamu watapewa kinywaji kimoto mwisho wa umoto, na adhabu chungu mno kwa sababu ya kufuru zao.

71 Waambie hawa makafiri kwa kuwasibabi: Je, inasihhi kuwa tumuabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, asiye weza kutuletea nafuu wala dhara? Na turejee kwenye shirki baada ya kuwa Mwenyezi Mungu kesho tupa tawfiqi ya kufikia Imani? Na tuwe kama aliye zugwa na mashetani na wakampoteza katika ardhi, akawa yuko katika pweleo lisilo weza kumwongoa kufuata Njia iliyo nyooka, na hali anao marafiki walio ongoka nao wanajaribu kumwokoza atoke kwenye upotofu, huku wakisema: Rejea kwenye njia yetu iliyo sawa; naye akawa hawaitikii!! Sema ewe Nabii: Hakika Uislamu ndio uwongofu na ndio uwongozi, na vyenginevyo ni upotofu tu. Na Mwenyezi Mungu ametuamrisha tuufuate Uislamu. Naye ndiye Muumba wa viumbe vyote, na ndiye Mwenye kuviruzuku, na Mwenye kupanga mambo yao.

72 Waachilieni mbali hao washirikina baada ya kuwa mmewaita kwenye uwongofu, na nendeni kwenye ibada ya Mola wenu Mlezi. Na timizeni Sala kwa njia ya unyenyekevu ulio kamilika kabisa. Na mkhofuni Mwenyezi Mungu, na timizeni amri zake. Kwani kwake Yeye ndio mtakusanywa nyote nyinyi.

73 Na ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi, na akasimamia uumbaji wake kwa Haki na hikima. Na wakati wowote Mwenyezi Mungu akitaka kiwe kitu kinakuwa papo hapo. Vitu huwa kwa neno: "Kuwa". Na kila neno lake ni la kweli na la haki. Na Yeye peke yake ndiye Mwenye uweza wa kutenda usio na ukomo Siku ya Kiyama, siku litapo pulizwa barugumu la kutangazwa ufufuo. Naye, *Subhanahu*, ndiye Mwenye kutulia juu ya ujuzi wake wa mambo yaliyo fichikana na yanayo onekana. Na ndiye anaye endesha mambo yake yote kwa hikima, na ndiye Mwenye kukusanya katika ujuzi wake mambo yaliyo fichikana na mambo yaliyo dhihiri.

74 Na ewe Nabii! Kumbuka yaliyo kuwa pale Ibrahim alipo mwambia baba yake, Azar, naye ameuadhika naye kwa kuwaabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu: Haikufalii wewe kuyafanya masanamu kuwa ni miungu. Hakika mimi nakuona wewe na kaumu yako walio nawe katika ibada hii, ni dhaahiri kuwa mko mbali na Njia ya Haki.

75 Kama alivyo ona Ibrahim - kwa tawfiqi yetu - upotovu wa watu wake katika kuyafanya masanamu ndio miungu, kadhaalika tumemwonyesha ufalme wetu mkubwa wa mbinguni na duniani na vilio humo, ili aweze kusimamisha hoja kwa watu wake, na ili azidi kuamini.

76 Ibrahim alimwomba Mola wake Mlezi, naye Mwenyezi Mungu akamhidi. Usiku ulipo kuja ukauziba

77. Alipo uona mwezi unachomoza alisema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu. Ulipotua akasema: Kama Mola Mlezi wangu hakuniongoa, nitakuwa katika kaumu walio potea.⁷⁷

78. Na alipo liona jua linachomoza akasema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu. Huyu mkubwa kuliko wote. Lilipo tua, alisema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayo fanyia ushirikina.⁷⁸

79. Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa kwa aliye ziumba mbingu na ardhi, wala mimi si miongoni mwa washirikina.⁷⁹

80. Na watu wake wakamhoji. Akasema: Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ameniongoa? Wala siogopi hao mnao washirikisha naye, ila Mola wangu Mlezi akipenda kitu. Mola wangu Mlezi amekusanya ilimu ya kila kitu. Basi je, hamkumbuki?⁸⁰

81. Na vipi nivikhofu hivyo mnavyo vishirikisha, hali nyinyi hamkhofu kuwa nyinyi mmemshirikisha Mwenyezi Mungu na kitu ambacho hakukiteremshia uthibitisho. Basi kundi gani katika mawili haya lina haki zaidi kupata amani, kama nyinyi mnajua?⁸¹

82. Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakao pata amani na wao ndio walio ongoka.⁸²

83. Na hizo ndizo hoja zetu tulizo mpa Ibrahim kuhojiana na watu wake. Tunamnyanyua kwa vyeo tumtakaye. Hakika Mola Mlezi wako ni Mwenye hikima na Mwenye ujuzi.⁸³

mchana kwa kiza chake, akaona nyota inameremeta. Akasema: Huyu ndiye Mola wangu Mlezi. Ilipo potea, akasema kwa kuukataa ungu wa nyota: Sikubali kuabudu miungu inayo ondoka na kugeuka!

77 Alipo uona mwezi umechomoza baada ya hayo, akasema akijiambia mwenyewe: Huyu ndiye Mola wangu Mlezi. Ulipo ondoka mwezi, na kukadhihiri kuvunjika ungu wake, akasema ili kuzielekeza nafsi zao ziombe hidaya: Ninaapa, kama Mola Mlezi wangu hakunihidi kwenye Haki, basi hapana shaka nitakuwa katika watu wanao babaika, (wasio jua mojawo la kulishika).

78 Tena baada ya hayo, akaliona jua linachomoza. Akasema: Huyu ndiye Mola Mlezi wangu, kwani huyu ni mkubwa kuliko nyota zinavyo onekana. Lilipo kuchwa, likapotea, akasema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika kumshirikisha kwenu Mwenyezi Mungu na masanamu kwa kuyaabudu.

79 Alipo kwisha ona udhaifu wa viumbe alimuelekea aliye viumba, akisema: Mimi nimeyaelekeza makusudio yangu kwa kumuabudu Mwenyezi Mungu pekee, ambaye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi. Nimejitenga na kila njia isipo kuwa Njia yake Yeye tu. Wala mimi, baada ya nilivyo kwisha ona dalili za Tawhidi (Umoja wa Allah), si katika wanao ridhia kuwa miongoni mwa washirikina kama wao.

80 Na juu ya hivyo, watu wake walijadiliana naye katika Umoja wa Mwenyezi Mungu, na wakamtisha kuwa atapata ghadhabu ya miungu yao. Basi yeye akawaambia: Haikufaliini nyinyi kuzozana nami katika Umoja wa Mwenyezi Mungu, naye amekwisha nihidi kufikia Haki. Wala siogopi ghadhabu ya miungu yenu mnayo ifanya ni washirika wa Mwenyezi Mungu. Lakini Mola wangu Mlezi akipenda madhara yatatokea, kwa kuwa Yeye pekee ndiye Muweza. Naye Mola wangu Mlezi amekusanya ilimu ya vitu vyote, na hao miungu yenu haina chochote inacho jua! Je, mmeghafilika na yote hayo, na hamtambui kuwa mjinga aliye emewa hastahiki kuabudiwa?

81 Na katika ajabu ni kuwa mimi niogope hiyo miungu yenu ya uwongo, na nyinyi hamna khofu kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu iliyo simama ushahidi wa Umoja wake, nyinyi mna shiriki kuabudu vitu ambavyo havina ushahidi kuwa vinastahiki kuabudiwa. Basi katika hali hii kikundi gani baina ya sisi chenye haki ya utulivu na amani, ikiwa kweli nyinyi mnajua Haki na mnaaitambua?

82 Wanao muamini Allah, (Mwenyezi Mungu), na wasiichanganyishe imani yao hii na ibada ya yeyote asiye kuwa Yeye - hao tu ndio wenye haki ya kupata utulivu, na ni wao tu ndio walio ongoka kuishika Njia ya Haki na Kheri.

83 Na hiyo hoja kubwa ya Ungu wetu, na Umoja wetu, tulimpa Ibrahim aisimamisha kupambana na watu wake, naye kwa hiyo akatukuka juu yao. Na mtindo wetu kwa waja wetu ni kuwa tunamnyanyua madaraja kwa ujuzi na hikima tumpendaye katika wao. Hakika Mola Mlezi wako, ewe Nabii, ni Mwenye hikima. Huweka kila kitu pahala pake. Ni Mwenye kuwajua wepi wanastahiki kutukuzwa, na wepi hawastahiki.

- 84.** Na tukamtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaakub. Kila mmoja wao tulimwongoa. Na Nuhu tulimwongoa kabla. Na katika kizazi chake tulimwongoa Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo tunavyo walipa wafanyao wema.⁸⁴
- 85.** Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas. Wote walikuwa miongoni mwa watu wema.⁸⁵
- 86.** Na Ismail, na Al Yasaa, na Yunus, na Lut'. Na wote tuliwafadhilisha juu ya walimwengu wote.⁸⁶
- 87.** Na kutokana na baba zao, na vizazi vyao na ndugu zao. Na tukawateuwa na tukawaongoa kwenye Njia iliyo nyooka.⁸⁷
- 88.** Hiyo ni hidaya ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo humhidi amtakaye katika waja wake. Na lau wangelimshirikisha yangelimwaharibikia waliyo kuwa wakibatenda.⁸⁸
- 89.** Hao ndio tulio wapa Vitabu na hukumu na Unabii. Ikiwa hawa watayakataa hayo, basi tumekwisha yawakilisha kwa watu wasio yakataa.⁸⁹
- 90.** Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewahidi. Basi fuata hidaya yao. Sema: Mimi sikuombeni ujira. Haya hayakuwa ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.⁹⁰
- 91.** Na hawakumkadiria Mwenyezi Mungu kwa haki ya kadri yake, walipo sema: Mwenyezi Mungu hakumteremshia mwanaadamu chochote. Sema: Nani aliyo teremsha Kitabu alichokuja nacho Musa, chenye nuru na uwongofu kwa watu, mlicho kifanya kurasa kurasa mkizionyesha, na mengi mkiyaficha. Na mkafunzwa mlilo kuwa hamyajui nyinyi wala baba zenu? Sema: Mwenyezi Mungu. Kisha waache wacheze katika porojo lao.⁹¹

84 Na Sisi tulimpa Ibrahim, Is-haq na Yaaqub bin Is-haq. Na tukamwezesha kila mmoja wao kufikia Haki na Kheri, kama baba yao. Na kabla yake tulimwezesha Nuhu hivyo hivyo, na tukawaongoa katika wazao wa Nuhu, Daud, na Suleiman, na Ayyub, na Yusuf, na Musa, na Harun. Kama tulivyo walipa hawa, tunawalipa wafanyao wema kwa wanavyo stahiki.

85 Na tuliwaongoa Zakariya, na Yahya, na Isa, na Ilyas - kila mmoja wao katika hawa ni miongoni mwa waja wetu walio wema.

86 Na tuliwaahidi Ismail, na Alyasaa, na Yunus, na Lut'; na tukawafadhilisha kila mmoja wa hawa wote kushinda walimwengu wote wa zama zao, kwa kuwapa uwongofu na Unabii.

87 Na tuliwateuwa baadhi ya mababa wa hao, na dhuriya zao, na ndugu zao, na tukawakhitari wao, na tukawawezesha waifuata Njia isiyo kwenda upogo.

88 Hiyo ndiyo tawfiqi kubwa waliyo ipata watu hawa, nayo ni tawfiqi (uwezesho) iliyo tokana na Mwenyezi Mungu, ambayo humwafiqia (humwezesha) amtakaye katika waja wake. Na lau wangelimshiriki watu hawa walio khitariwa zingeli potea a'mali zao za kheri zote walizo zifanya, na wasingeli pata thawabu.

89 Hao ndio tulio wapa Vitabu vilivyo teremshwa, na ilimu zenye manufaa, na utukufu wa Unabii. Na washirikina wa Makka wakiyapinga mambo haya matatu, basi wamekwisha ahidiwa watu wengine wasio yakataa hayo wayachunge na wanafike kwayo.

90 Hao ndio Mwenyezi Mungu amewawezesha kuishika Njia ya Haki na kheri. Basi nyinyi wafuateni hao katika mambo waliyo wafikiana kwayo, nayo ni mambo ya misingi ya Dini, na misingi ya mwendo mwema, wala msifuate njia nyengine isiyo kuwa yao... Ewe Nabii! Waambie watu wako kama wao hawa walivyo waambia watu wao: Sitaki kwenu ujira kwa ajili ya kulifikisha Neno la Mwenyezi Mungu! Hii Qur'ani si chochote ila ni Ukumbusho kwa walimwengu wote, wala sina lengo mimi ila kuwa nyinyi mnafike na hii Qur'ani.

91 Na hawa makafiri hawakumkadiria Mwenyezi Mungu na rehema yake na hikima yake kwa anavyo stahiki, walipo kanya kuteremshwa ujumbe wake kwa binaadamu yeyote! Ewe Nabii! Waambie washirikina na wanao waunga mkono katika hayo miongoni mwa Mayahudi: Nani aliye kiteremsha Kitabu alichokuja nacho Musa, ambacho kina nuru iliyo zaga, na uwongofu wa kuongozea? Nyinyi Mayahudi mnakifanya hicho kuwa ni maandiko yaliyo gawiwa mafungu mbali mbali. Yanayo kubaliana na mapendo yenu mnayaonyesha, na mengi mnayaficha yale yanayo kupelekeeni kuiamini na kuisadiki

92. Na hiki ni Kitabu tulicho kiteremsha, kilicho barikiwa, chenye kuhakikisha yaliyo tangulia, na ili uwonye Mama wa Miji na walio pembezoni mwake. Na wenye kuamini Akhera wanakiamini hichi, nao wanazihifadhi Sala zao.⁹²

93. Nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye mzuliya uwongo Mwenyezi Mungu, au anaye sema: Mimi nimeletewa wahyi; na hali hakuletewa wahyi wowote. Na yule anaye sema: Nitateremsha kama alivyo teremsha Mwenyezi Mungu. Na lau ungeli waona madhaalimu wanavyo kuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyooshea mikono wakiwambia: Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya mliyo kuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyo ya haki, na mlivyo kuwa mkizifanyia kiburi Ishara zake.⁹³

94. Nanyi mlitujia wapweke kama tulivyo kuumbeni mara ya kwanza. Na mkayaacha nyuma yenu yote tuliyo kupeni, na wala hatuwaoni hao waombezi wenu, ambao mlidai kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu kwenu. Yamekatika makhusiano baina yenu, na yamekupoteeni mliyo kuwa mkidai.⁹⁴

95. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye mpasujaji mbegu na kokwa, zikachipua. Humtoa aliye hai kutoka maiti, naye ni mtoaji maiti kutokana na aliye hai. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu. Basi vipi mnageuzwa?⁹⁵

Qur'ani. Na kutokana na Kitabu hicho mmejifunza mambo ambayo nyinyi na baba zenu hamkuwa mkiyajua!! Na ewe Nabii! Jawabu wape wewe kwa kuwambia: Mwenyezi Mungu ndiye aliye iteremsha Taurati. Kisha waache wakiendelea katika upotovu, wakicheza kama watoto wadogo.

92 Na hii Qur'ani tumeiteremsha - kama tulivyo iteremsha Taurati - ina kheri nyingi, na itabaki mpaka Siku ya Kiyama. Inasadikisha Vitabu vilivyo teremshwa mbele yake, inaeleza khabari ya kuteremkwa kwao, ili iwape bishara Waumini, na iwakhofishe makafiri wa Makka na pembezoni mwake pande zote za dunia juu ya ghababu ya Mwenyezi Mungu, ikiwa hawakuifuata. Na wale wanao isadiki Siku ya malipo, kule kutaraji kwao thawabu na kukhofu adhabu, kunawapelekea kuiamini hii Qur'ani. Na kwa hivyo wao wanahifadhi kutekeleza Sala kwa ukamilifu na utimilivu.

93 Nabii huyu hakusema uwongo alipo tangaza kuwa Qur'ani imetoka kwa Mwenyezi Mungu. Na hapana mwenye kumshinda kwa udhaalimu huyo aliye mzulia uwongo Mwenyezi Mungu, au akasema: Nimepata wahyi (ufunuo) kutoka kwa Mwenyezi Mungu, bila ya kuwa kapata wahyi wowote ule. Vile vile hapana dhaalimu mkubwa zaidi kuliko anaye sema: Mimi nitaleta maneno sawa na hayo aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu! Na lau kuwa unajua hali ya hao madhaalimu nao wamo katika shida za mauti, na Malaika wanazing'oa roho zao kutokana na miili yao, kwa ukali na nguvu, ungeli ona vitisho vya kushitua vinawashukia! Wakati huo hao huambiwa: Sasa malipo yenu ya adhabu ya kudhalilisha na kufedhehesha yanaanza. Malipo haya ni kwa vile mlivyo kuwa mkimzulia Mwenyezi Mungu bila ya haki, na ni malipo kwa kuwa kiburi chenu kilikuzuieni msiangalie na kuzipima Aya, Ishara, za uumbaji za Mwenyezi Mungu ziliomo katika Qur'ani.

94 Na Mwenyezi Mungu atawaambia Siku ya Kiyama: Sasa bila ya shaka mmekwisha yakinisha kwa nafsi zenu kuwa kweli mmefufuliwa kutoka makaburini kwenu, kama tulivyo kuumbeni mara ya kwanza. Na mmetujia hali ni wapweke, hama mali, wala watoto, wala marafiki. Na mmeviacha nyuma yenu vyote tulivyo kupeni na mkaghurika navyo. Na wala Sisi hatuwaoni pamoja nanyi hao waombezi ambao mlidai kuwa watakunusuruni kwa Mwenyezi Mungu, na kuwa wao ati ni washirika wa Mwenyezi Mungu katika ibada! Makhusiano yote baina yenu na wao yamekwisha katika, na yamekupoteeni mliyo kuwa mkidai kuwa yatakufaeni.

95 Hakika dalili za uwezo wa Mwenyezi Mungu kufufua, na kuwa ni Yeye pekee anaye stahiki kuabudiwa, na kufufua kwake watu kutoka makaburini, zimeenea na zimo za namna mbali mbali. Kwani ni Yeye pekee yake ndiye anaye ipasua mbegu ukachipua mmea, na ni Yeye ndiye anaye ipasua kokwa ukatokeza mti. Na hivyo humfufua aliye hai kutokana na kisicho kuwa hai, kama mtu kutokana na udongo. Na akatoa kisicho kuwa hai kutokana na kilicho hai, kama maziwa kutokana na mnyama. Huyu Muweza Mtukufu ndiye Mungu wa Haki. Basi kisiwepo kitu cha kukugeuzeni mkaacha kumuabudu Yeye mkaviabudu vyenginevyo.. (Tazama Maelezo 6:95)

96. Ndiye anaye pambazua mwangaza wa asubuhi; na ameufanya usiku kwa mapumziko na utulivu, na jua na mwezi kwenda kwa hisabu. Hayo ndiyo makadirio ya Aliye tukuka Mwenye nguvu, Mwenye ujuzi.⁹⁶

97. Na Yeye ndiye aliye kuwekeeni nyota ili mwongoke kwazo katika kiza cha bara na bahari. Hakika tumezichambua Ishara hizi kwa watu wanao jua.⁹⁷

98. Na Yeye ndiye aliye kuzalisheni kutokana na nafsi moja. Pako pahali pa kutulia na pa kupita njia. Hakika tumezichambua Ishara hizi kwa watu wanao fahamu.⁹⁸

99. Na Yeye ndiye anaye teremsha maji kutoka mbinguni; na kwayo tunatoa mimea ya kila kitu. Kutokana na baadhi yao tukatoa mimea ya majani, tukatoa ndani yake punje zilizo pandana; na kutokana na mitende yakatoka kwenye makole yake mashada yaliyo inama; na bustani za mizabibu na mizaituni, na makomamanga, yaliyo fanana na yasiyo fanana. Angalieni matunda yake yanapo zaa na yakawiva. Hakika katika hayo pana Ishara kwa watu wanao amini.⁹⁹

100. Bado wamemfanyia Mwenyezi Mungu majini kuwa washirika wake, na hali Yeye ndiye aliye waumba. Na wakamzulia, bila ya ujuzi wowote, kuwa ana wana wa kiume na wa kike. *Subhanahu*, Ametakasika na ametukuka juu ya hayo wanayo mbandikiza nayo!¹⁰⁰

101. Yeye ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi bila ya ruwaza. Itakuwaje awe na mwana naye hakuwa na mke? Naye ndiye aliye umba kila kitu. Naye ni Mwenye kujua kila kitu.¹⁰¹

96 Ni Yeye ndiye anaye toa mwangaza wa mchana kutokana na giza- giza la asubuhi, ili vilivyo hai viende kupata njia za maisha yao. Na akaufanya usiku uwe ni wa mapumziko ya mwili na roho, na akaufanya mwendo wa jua na mwezi wende kwa mpango mzuri kabisa ili watu wajue nyakati za ibada zao na maisha yao. Huo ndio mpango ulio fanywa kwa hikima, ndio tadbiri ya Mwenye uwezo Mwenye kuumiliki ulimwengu, Mwenye kukusanya kila kitu katika ujuzi wake.

97 Yeye ndiye aliye kufanyieni nyota zikuongozeni kwa zilivyo pangwa mfike mwendako, nanyi mnakwenda kizani usiku, bara au baharini. Hakika Sisi tumezibainisha dalili za rehema yetu, na uwezo wetu, kwa ajili ya watu ambao wanao nufaika kwa ilimu.

98 Yeye ndiye aliye kutoeni kwenye asli moja, nayo ni baba wa watu wote, Adam. Na Adam ametoka kwenye ardhi. Basi ardhi ndio kituo chenu muda wa uhai wenu, na ndipo pahala pa kupaaga baada ya kufa kwenu, na mkapotea chini yake. Na tumezibainisha dalili za uwezo wetu kwa watu wanao zingatia na kufahamu mambo yalivyo.

99 Naye ndiye anaye teremsha kutoka mawinguni maji, ambayo kwayo akatoa kila namna ya mimea. Kuna mimea inayo toa majani laini kuwa ni mboga, na tunatoa pia mimea ya kuzaa punje nyingi zimepandana wenyewe kwa wenyewe. Na kutokana na makole ya mitende mna mashada yamebeba tende, wepesi kuzipata. Na pia tumetoa kutokana na maji mizabibu, na zaituni, na makomamanga. Katika hiyo yapo matunda yalio fanana kwa sura, na yasiyo fanana kwa utamu, na harufu, na namna ya faida yake. Hebu yaangalieni kwa kupima na kuzingatia matunda yake inapo zaa hiyo miti, na matunda yanapo wiva, vipi yanapo komaa baada ya kupitia hali mbali mbali! Hakika katika haya zipo ishara kwa wanao itafuta Haki na wanaamini na kunyenyekea. (*Tazama* Maelezo 6:99)

100 Juu ya dalili hizi makafiri wamewafanya Malaika na mashetani ni washirika wa Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ndiye aliye waumba hao. Haiwafalii kujua hayo wakamuabudu asiye kuwa Yeye, naye ndiye aliye waumba Malaika na mashetani. Haitakikani wawaabudu hao nao wameumbwa kama wao!! Na hawa makafiri wakambunia Mwenyezi Mungu wana. Wakristo wakadai kuwa Masihi ni mwana wa Mungu, na baadhi ya washirikina wa Kiarabu wakadai kuwa Malaika ni mabinti wa Mwenyezi Mungu. Na huo ni ujinga, kutokuwa na ilimu! Mwenyezi Mungu Mtukufu ameepukana na hayo wanayo muambatisha naye *Subhana*.

101 Mwenyezi Mungu, ambaye ameziumba mbingu na ardhi bila ya kuwa na kiigizo kilicho tangulia, vipi awe na mwana, kama wanavyo dai hawa, na hali Yeye hana mke, naye ndiye aliye umba vitu

- 102.** Huyo ndiye Allah, Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu, hapana mungu ila Yeye, Muumba wa kila kitu. Basi muabuduni Yeye tu. Naye ni Mtegemewa wa kila kitu.¹⁰²
- 103.** Macho hayamfikilii bali Yeye anayafikilia macho. Naye ni Mjuzi, Mwenye khabari.¹⁰³
- 104.** Zimekwisha kukujieni hoja wazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Basi anaye ona ni kwa faida yake mwenyewe, na anaye pofuka basi ni khasara yake. Nami si mtunzaji wenu.¹⁰⁴
- 105.** Na namna hivyo tunazisarifu Aya, na wao wakwambie: Umesoma. Na ili tuyabainishe kwa watu wanao jua.¹⁰⁵
- 106.** Fuata uliyo funuliwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Hapana mungu ila Yeye. Na jitenge na washirikina.¹⁰⁶
- 107.** Na lau Mwenyezi Mungu angeli penda, wasingeli shiriki. Na Sisi hatukukufanya wewe uwe mtunzaji wao. Wala wewe si mlinzi juu yao.¹⁰⁷
- 108.** Wala msiwatukane hao wanao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, wasije na wao wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua. Namna hivyo tumewapambia kila umma vitendo vyao. Kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao Mlezi, naye atawaambia waliyo kuwa wakiyatenda.¹⁰⁸
- 109.** Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu kwa ukomo wa viapo vyao, kuwa ikiwafikia Ishara wataimini. Sema: Ishara ziko kwa Mwenyezi Mungu. Na nyinyi hamjui kuwa

vyote? Miongoni mwa vitu hivyo ni hao wanao wafanya washirika wake. Naye ni Mjuzi wa kila kitu, na anawahisabia wasemayo na watendayo, na ni Mwenye kuwalipa kwa kauli yao na vitendo vyao.

102 Huyo aliye sifika kwa sifa za ukamilifu ndiye Allah, Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu, ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye, Muumba wa kila kitu vilivyo kuwako, na vitavyo kuwa. Basi ni Yeye tu Mwenye kustahiki kuabudiwa. Basi muabuduni Yeye, na Yeye peke yake ndiye Mwenye kutawala kila kitu na kila jambo. Marejeo yote ni kwake tu.

103 Macho hayamuoni dhati yake, na Yeye anajua undani wa macho na vyenginevyo. Naye ni Mjuzi hakimpotei kitu, ni Mwenye khabari za kila kitu.

104 Ewe Nabii! Waambie watu: Zimekwisha kujieni kutoka kwa Muumba wenu na Mwenye kumiliki mambo yenu yote, hoja na maelezo wazi katika hii Qur'ani. Hizo zinakuangazi ni Njia ya Haki. Basi mwenye kunafiika kwazo, manufaa ni yake mwenyewe. Na mwenye kujitenga nazo, basi amejidhuru mwenyewe! Wala mimi si mlinzi wenu, bali mimi ni Mjumbe ninakufikishieni niliyo tumwa kwenu.

105 Na mfano wa uchambuzi kama huu wa pekee katika kueleza dalili za maumbile, ndivyo tunavyo eleza Ishara zetu katika Qur'ani kwa njia namna kwa namna na kwa mbali mbali, ili kusimamisha hoja za kuwashinda hao wapingao. Kwa hivyo wao hawapati ila kuzua uwongo, wakakutuhumu kuwa haya umejifunza kwa watu, wala hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu. Nasi tunabainisha haya uliyo teremshiwa, nayo ni Haki isiyo athirika na kipendacho moyo, kwa ajili ya watu ambao wanayoielewa Haki na wanainyenyekea.

106 Ewe Nabii! Fuata wahyi ulio kujia kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye kumiliki na kuendesha mambo yako. Hakika Yeye peke yake ndiye Mungu anaye stahiki kut'iwa na kunyenyekewa. Basi shikamana na ut'iifu wake, wala usibali inadi za washirikina.

107 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka wamuabudu Yeye peke yake angeli walazimisha kwa nguvu na kwa uweza wake. Lakini Yeye amewaachilia watumie khiari yao. Na Sisi hatukukufanya wewe kuwa ni muangalizi wao, ukiwahisabia vitendo vyao. Wala wewe hukulazimisha kuwa usimamie kuwapangia na kuwatengenezea mambo yao.

108 Enyi Waumini! Msiyatukane masanamu ya washirikina wanayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu, isije chuki yao kwa hayo ikawapelekea hasira ya kumtukana Mwenyezi Mungu kwa uadui na ujinga. Kama tulivyo wapambia hawa kupenda masanamu yao, kila umma una a'mali yake kwa mujibu wa makdara yao. Na marejeo ya wote ni kwa Mwenyezi Mungu peke yake Siku ya Kiyama. Naye atawaeleza khabari ya vitendo vyao, na atawalipa kwavyo.

zitapo kuja hawato amini.¹⁰⁹

110. Nasi twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyo kuwa hawakuamini mara ya kwanza, tunawaacha katika maasi yao wakitangatanga.¹¹⁰

111. NA LAU kuwa tungeli wateremshia Malaika, na maiti wakazungumza nao, na tukawakusanyia kila kitu mbele yao, bado wasingeli amini, ila Mwenyezi Mungu atake. Lakini wengi wao wamo ujingani.¹¹¹

112. Na kadhaalika tumemfanyia kila Nabii maadui mashet'ani wa kiwatu, na kijini, wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba-pamba, kwa udanganyifu. Na angeli penda Mola wako Mlezi wasingeli fanya hayo. Basi waache na wanayo yazua.¹¹²

113. Na ili nyoyo za wasio amini Akhera zielekee hayo, nao wayaridhie na wayachume wanayo yachuma.¹¹³

114. Je, nimtafute hakimu ghairi ya Mwenyezi Mungu, naye ndiye aliye kuteremshieni Kitabu kilicho elezwa waziwazi? Na hao tulio wapa Kitabu wanajua ya kwamba kimeteremshwa na Mola wako Mlezi kwa Haki. Basi usiwe katika wanao tia shaka.¹¹⁴

115. Na yametimia maneno ya Mola Mlezi wako kwa kweli na uadilifu. Hapana awezaye kuyabadilisha maneno yake. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.¹¹⁵

109 Na washirikina waliapa ukomo wa viapo vyao, kuwa ikiwajia Ishara ya kuiona katika Ishara walizo zitaka, basi yakini hiyo itakuwa ni sababu ya kuamini kwao. Sema ewe Nabii: Ishara hizi ziko kwa Mwenyezi Mungu. Yeye peke yake ndiye Mwenye madaraka juu yake hizo ishara. Mimi sina uweza wa hayo. Nyinyi Waumini, hamjui ninayo yajua Mimi. Hata zikiwajia Ishara hizi hawataamini.

110 Na nyinyi pia hamjui kuwa Sisi tumezigeuza nyoyo zao zinapo kuja Ishara huzitafutia visababu na tafsiri, na tunayageuza macho yao kwa mambo ya dhana na mawazo tu. Kwa hivyo baada ya kuja Ishara hali yao inakuwa kama mwanzo. Nasi tunawawacha wakipotea katika dhulma yao na inadi yao.

111 Hakika hao walio apa kuwa ikiwajia Ishara wataiamini, ni waongo. Mwenyezi Mungu anajua vilivyo imani yao. Lau kuwa sisi tungeli teremsha Malaika wakawaona kwa macho, na maiti wakawasemeza baada ya kufufuliwa makaburini mwao, na kuwakusanyia kila kitu mbele yao kikiwakabili na kuwabainishia haki, bado wasingeli amini ila akipenda Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa waamini. Na wengi hawaitambui Haki wala hawafuati, kwa sababu nyoyo zao zimesibiwa na upofu wa kijahiliya.

112 Kama ilivyo kuwa hao wamekufanyia uadui na inadi, na hali wewe unataka kuwaongo, basi kadhaalika tumemfanyia kila Nabii anaye peleka ujumbe wetu, maadui katika wanaadamu majeuri na majini majeuri, ambao wanajificha kwako na huwaoni, wakitiliana wasiwasi kwa maneno ya kupamba-pamba na udanganyifu, yasiyo na ukweli. Basi kwa hayo huingiza ghururi kwa uwongo! Na hayo yote ni kwa kudra ya Mwenyezi Mungu na kutaka kwake. Na lau angeli taka wasingeli fanya hayo. Lakini hayo ni kwa ajili ya kuzisafisha nyoyo za Waumini. Basi waachilie mbali hao walio potea na kufuru zao za maneno yao wanayo yazua.

113 Wao huyapindua maneno ya upotovu wazidanganye nafsi zao na ziridhie, na zielekee huko huko vile vile nyoyo za walio kama wao majeuri wasio iogopa Akhera, wanao itakidi kuwa uhai ni dunia tu, na waingie katika madhambi na maasi kwa sababu ya kuto iamini kwao Siku ya Akhera.

114 Ewe Nabii! Waambie: Hii ni hukumu ya Mwenyezi Mungu kwa Haki, iliyo bainishwa na Aya zilizo zagaa. Basi haijuzu nitaafute hukumu isiyo kuwa yake Yeye ya kutupambanua baina yangu na nyinyi. Mwenyewe Subhana kesho hukumu, na ameteremsha Kitabu kitukufu kiwe ni hoja juu yenu. Nanyi mmshindwa kuleta mfano wake. Nacho kinabainisha Haki na uadilifu. Na wale walio pewa Kitabu wanajua kuwa hii Qur'ani imetoka kwa Mwenyezi Mungu, na imekusanya Haki, kama vilivyo bashiri vitabu vyao, ijapo kuwa wanajaribu kuyaficha hayo. Basi wewe Nabii, pamoja na walio kufuata, msiwe katika wenye kutilia shaka Haki baada ya kubainishwa kwake.

115 Na hakika hukumu ya Mwenyezi Mungu imekwisha toka. Basi maneno ya Mola wako Mlezi ya kweli na ya uadilifu yametimia kwa kuteremshwa Kitabu hichi Kitukufu, chenye kukusanya ukweli. Na ndani imo mizani ya kweli ya kupimia Haki na upotovu. Wala hapana wa kuyageuza maneno ya Mwenyezi Mungu na Kitabu chake. Naye Subhana ni Mwenye kusikia kila lisemwalo, Mwenye kukijua kila kinacho

116. Na ukiwat'ii wengi katika hawa waliomo duniani watacupoteza na Njia ya Mwenyezi Mungu. Hawa hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kusema uwongo tu.¹¹⁶

117. Hakika Mola wako Mlezi ndiye Mjuzi kushinda wote kuwajua walio potea Njia yake, na ndiye Mjuzi kushinda wote kuwajua walio hidika.¹¹⁷

118. Basi kuleni katika walio somewa jina la Mwenyezi Mungu, ikiwa mnaziamini Aya zake.¹¹⁸

119. Na kwa nini msile katika walio somewa jina la Mwenyezi Mungu, naye amekwisha kubainishieni alivyo kuharimishieni, isipo kuwa vile mnavyo lazimishwa? Na hakika wengi wanapoteza kwa matamano yao bila ya kuwa na ilimu. Hakika Mola wako Mlezi ndiye Mjuzi kushinda wote kuwajua wanao pindukia mipaka.¹¹⁹

120. Na acheni dhambi zilizo dhaahiri na zilizo fichikana. Hakika wanao chuma dhambi watalipwa kwa waliyo kuwa wakiyachuma.¹²⁰

121. Wala msile katika wale wasio somewa jina la Mwenyezi Mungu. Kwani huo ni upotofu. Na kwa yakini mashet'ani wanawafunza marafiki zao kubishana nanyi. Na mkiwafuata basi hapana shaka nyinyi mtakuwa washirikina.¹²¹

122. Je, aliye kuwa maiti kisha tukamhuisha, na tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu, mfano wake ni kama aliyoko gizani akawa hata havezi kutoka humo?

toka kwao.

116 Na ikiwa *Subhanahu* ndiye mwenye hukumu ya uadilifu inayo rejewa kwenye Vitabu vyake katika kutafuta Haki na kuijua, basi ewe Nabii, usiwe wewe na walio pamoja nawe, mkamfuata yeyote anaye achana na kauli ya Haki, hata ikiwa hao ni wengi wa idadi. Kwani ukiwafuata aghlabu ya watu ambao hawategemei Sharia iliyo teremshwa na Mwenyezi Mungu, watakuweka mbali na Njia ya Haki iliyo nyooka. Na hiyo ndiyo Njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na watu hao hawendi ila nyuma ya dhana na mawazo tu, na wala hawasemi ila kwa kukisia tu; hawategemei hoja na ushahidi.

117 Na hakika Mola wako Mlezi ndiye Mwenye kujua kwa ujuzi ambao hapana mfano wake, kuwajua hao ambao wamekuwa mbali na Njia ya Haki, na hao ambao wameongoka na uwongofu ukawa ndio sifa yao.

118 Ilivyo kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye anaye wajua walio hidika na walio potea, basi msielekee kwenye upotovu wa washirikina wa kuharimisha baadhi ya nyama hoa (nyama wa kufuga). Basi kuleni katika hao, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu amekuruzukuni hao, na amewafanya ni halali na wazuri, na hapana madhara kuwala. Na mnapo wachinja litajeni jina la Mwenyezi Mungu juu yao, maadamu nyinyi mnamuamini Yeye na mnamnyenyekea.

119 Na hakika hapana sababu yoyote au dalili ya kukuziieni kula nyama aliye tajiwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu juu yake wakati wa kuchinja miongoni mwa nyama hoa. (yaani nyama wa kufuga.) Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika na Aliye tukuka amekwisha kubainishieni vilio harimishwa, katika hali isiyo kuwa ya dharura, kama mzoga na damu (na nguruwe). Watu wengi wanaacha Haki, si kwa lolote, ila kufuata pumbao la nafsi zao tu, bila ya kuwa wamepewa ilimu, au hoja iliyo thibiti kwao. Kama hao Waarabu walio jiharimishia wenyewe baadhi ya wanyama wa kufuga. Wala nyinyi hamna makosa kwa kula kilicho zaliwa, bali wao ndio wamepita mipaka kwa kuharimisha kilicho halali. Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mjuzi wa hao walio pindukia mipaka kwa ujuzi usio na mfano wake kwa hakika.

120 Sio uhamngu kuharimisha alichu halalisha Mwenyezi Mungu. Hakika uhamngu ni kuacha madhambi ya nje na ndani. Basi wacheni madhambi katika vitendo vyenu, vinavyo onekana na vilivyo fichika. Na bila ya shaka wanao chuma madhambi watalipwa kwa kadri ya madhambi wayatendayo.

121 Ilivyo kuwa hao wanyama ni halali kwenu kwa kuwachinja, basi msile yule ambaye hakutajiwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati wa kumchinja, ikiwa limeachwa kutajwa makusudi, au limetajwa jina jingine lisilo kuwa la Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwani hivyo ni upotovu, na kutokana na hukumu ya Mwenyezi Mungu! Na hakika majeuji, Iblisi na wasaidizi wake, huwatia tia katika vifua vya wale walio kwisha watawala, ili wajadiliane nanyi kwa upotovu, na wakupelekeeni kuharimisha alivyo halalisha Mwenyezi Mungu. Nanyi mkiwafuata mtakuwa mfano wao katika kumshirikisha Mwenyezi Mungu.

Kama hivyo makafiri wamepambiwa waliyo kuwa wakiyafanya.¹²²

123. Kadhaalika katika kila mji tumewajaalia wakubwa wa wakosefu wao wafanye vitimbi ndani yake. Na wala hawafanyii vitimbi isipo kuwa nafsi zao, nao hawatambui.¹²³

124. Na inapo wajia Ishara, wao husema: Hatutoamini mpaka tupewe mfano wa walio pewa Mitume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi kuliko wote kujua wapi anaweka ujumbe wake. Itawafikia hao walio kosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyo kuwa wakivifanya.¹²⁴

125. Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na anaye taka apotee hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wasio amini.¹²⁵

126. Na hii ndiyo Njia ya Mola wako Mlezi Iliyo nyooka. Tumezipambanua Aya kwa watu wanao kumbuka.¹²⁶

127. Hao watapata nyumba ya salama kwa Mola Mlezi wao. Naye ndiye Rafiki Mlinzi wao kwa sababu ya waliyo kuwa wakiyatenda.¹²⁷

128. Na ile Siku atapo wakusanya wote awaambie: Enyi makundi ya majini! Hakika nyinyi mmechukua wafuasi wengi katika wanaadamu. Na marafiki zao katika wanaadamu waseme: Mola Mlezi wetu! Tulinufaishana sisi na wao. Na tumefikia ukomo wetu ulio tuwekea. Basi Mwenyezi Mungu atasema: Moto ndio makaazi yenu, mtadumu humo, ila apendavyo Mwenyezi Mungu. Hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye hikima, na Mwenye kujua.¹²⁸

122 Na nyinyi kwa Imani yenu si mfano wa washirikina hata kidogo. Basi haiwezi kuwa hali ya aliye kama maiti katika kupotea kwake, na Mwenyezi Mungu akampa nuru ya kuhidika, ambayo ni kama uhai, na akampa nuru ya Imani na hoja zilizo wazi, na kwa mwangaza wa nuru hiyo akaongoka na akawa anatembea nayo, haiwezi kuwa hali hiyo mfano wa hali ya ambaye kwamba anaishi katika giza lililo gubika. Na kama Mwenyezi Mungu alivyo ipamba Imani katika nyoyo za watu wa Imani, vile vile Shetani ameipamba shirki katika nafsi za madhaalimu wapinzani.

123 Ewe Nabii! Usistaajabu ukiwaona wakuu wa wakosefu katika Makka wanapanga njama za shari za kila namna! Kwani huo ndio mtindo wao katika kila mji mkubwa. Wakuu wa wakosefu wake huwa kazi yao kuzua vitimbi vya shari. Na malipo ya uovu wake utakuja waangukia wenyewe, lakini wao hawatambui wala hawahisi.

124 Hakika hawa wakuu wa wakosefu huwahusudu watu walio pewa na Mwenyezi Mungu ilimu, na Unabii, na uwongo. Basi ikiwajia hoja ya kukata hawaikubali, lakini husema: Hatuikubali Haki mpaka tuteremshiwe wahyi kama wanavyo teremshiwa Mitume. Na hali ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye ujuzi ambao haulingani na ujuzi wa mtu yoyote, kujua nani anaye stahiki kupata Utume wake. Ni Yeye ndiye anaye teua nani katika viumbe vyake ampe Utume wake. Hawa wenye inda, ikiwa wanataka ukubwa kwa inadi ya namna hii, basi watakuja pata unyonge na udhalili hapa duniani kwa sababu hiyo, na kesho Akhera watakuja pata adhabu kali kwa sababu ya huko kupanga kwao uwovu.

125 Ikiwa hao wamepotea, na nyinyi mkaongoka, basi ni kwa kutaka Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwa hukumu yake. Aliye muandikia hidaya humkunjulia kifua chake kwa nuru ya Uislamu. Na aliye muandikia kupotea kifua chake huwa na dhiki ya kweli kweli, kama kinavyo mbana kifua mwenye kupanda pahala pa juu, kama vile mbinguni. Pumzi humpaa, asiweze kitu! Na kwa hivi Mwenyezi Mungu huwaandikia ufasidi na kukatika tamaa hao ambao hawakujaaliwa kuwa na Imani katika shani yao. (*Tazama Maelezo 6:125*)

126 Na hii tuliyo ibainisha ndio Njia ya Haki Iliyo Nyooka. Nasi tumeipambanua na tumeiweka wazi kwa watu wote, na wala hawanufaiki kwayo ila wale ambao shani yao ni kukumbuka na kutaka hidaya.

127 Na hawa wanao kumbuka na wanao amini watapata Nyumba ya Amani, nayo ndiyo Pepo. Nao watakuwa chini ya ulinzi na urafiki wa Mwenyezi Mungu na mapenzi yake na nusra yake, kwa sababu ya mambo ya kheri waliyo yatenda duniani.

128 Na ilivyo kuwa wale walio ifuata Njia ya Mwenyezi Mungu Iliyo Nyooka watapata amani na ulinzi

129. Ndio kama hivi tunawaelekeza madhaalimu wapendane wao kwa wao kwa sababu ya waliyo kuwa wakiyachuma.¹²⁹

130. Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakukujieni Mitume kutokana na nyinyi wenyewe wakikubainishieni Aya zangu, na wakikuonyeni mkutano wa Siku yenu hii. Nao watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu. Na yaliwadanganya maisha ya dunia. Nao watajishuhudia wenyewe ya kwamba walikuwa makafiri.¹³⁰

131. Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola wako Mlezi hakuwa wa kuiangamiza miji kwa dhulma, hali wenyewe wameghafilika.¹³¹

132. Na wote wana daraja mbali mbali kutokana na yale waliyo yatenda. Na Mola wako Mlezi si mwenye kughafilika na yale wanayo yatenda.¹³²

133. Na Mola wako Mlezi ndiye Mkwasi, Mwenye rehema. Akipenda atakuondoeni na awaweke wengine awapendao badala yenu, kama vile alivyo kutoeni kutokana na uzazi wa watu wengine.¹³³

134. Bila ya shaka hayo mnayo ahidiwa yatafika tu, wala nyinyi hamtaweza kuyaepuka.¹³⁴

135. Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni muwezayo, na hakika mimi nafanya. Mtakuja

wa Mwenyezi Mungu, basi wale walio ifuata njia ya Shetani watapata malipo ya maasi waliyo yafanya hapo watapo kusanywa wote Siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu Aliye tukuka kwa Utukufu wake atawaambia hao majini na watu walio tenda dhambi: Enyi mlio kusanyika, katika majini hadi mmekithiri kuwapoteza watu, hata wamekufuateni wengi! Tena watasema wale watu walio wafuata: Ewe Muumba wetu na Mwenye kutusimamia! Hakika sisi kwa sisi tulipeana manufaa, na tukapeana starehe kwa matamano; na sasa ajali yetu uliyo tuwekea imekwisha fika. Hapo Mwenyezi Mungu Aliye tukuka kwa utukufu wake atasema: Makaazi yenu ya kukaa ni Motoni. Mtadumu humo milele, isipo kuwa Mwenyezi Mungu atakao penda kuwavua katika wale wasio kanya Ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Na hakika vitendo vya Mwenyezi Mungu daima vinakuwa kwa mujibu wa hikima na ujuzi.

129 Kama tulivyo wawacha waasi wa kibinaadamu na wa kijini wakistareheshana wao kwa wao, basi amewajaalia madhaalimu wawe ni marafiki wao kwa wao, kwa sababu ya madhambi makubwa wanayo yachuma.

130 Na Mwenyezi Mungu Mtukufu atawaambia Siku ya Kiyama: Enyi watu na majini! Mitume wamekujieni wakikutajieni hoja na dalili zilizo wazi, na wakikusomeeni Aya, na wakikuonyeni na mkutano wa Mwenyezi Mungu katika Siku yenu hii. Basi vipi mnakanusha? Nao watajibu: Tunakubali wenyewe madhambi tuliyo yatenda. Na maisha ya kidunia yaliwakhadaa kwa starehe zake, na wakajikiria nafsi zao kuwa hakika wao walikuwa wapinzani.

131 Na huku kutuma Mitume, wenye kuonya na kubainisha ni kwa kuwa Mola wako Mlezi, ewe Nabii, haiangamizi miji kwa dhulma yao na watu wake wameghafilika na Haki tu. Bali hapana budi ila awabainishie kwa uwazi na awaonye.

132 Na kila mtenda kheri au mtenda shari ana daraja yake ya malipo kwa anayo yatenda. Ikiwa kheri atapata kheri, na ikiwa shari basi atapata shari. Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika ndiye Muumba, si Mwenye kughafilika na wanayo yatenda. Bali hakika vitendo vyao vimo katika Kitabu kisicho acha dogo wala kubwa ila hulitia hisabuni.

133 Na Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola wako Mlezi, ni Mkwasi, hahitajii waja wala ibada zao. Na Yeye peke yake ndiye Mwenye rehema iliyo kusanya kila kitu. Na kwa mujibu wa hayo ndio akakuamrisheni mtende mema, na akakukatazeni maovu. Naye ndiye Muweza. Akitaka atakuondoeni na alete duniani wenginewe wa kufuatia baada yenu kwa mujibu wa atakavyo. Wala hilo si gumu kwake *Subhanahu*, Aliye takasika. Kwani Yeye alikuumbeni kutokana na uzao wa wengine walio kutangulieni. Nanyi mkawa ndio warithi wa ardhi baada yao.

134 Na hayo anayo kuonyeni kwayo, nayo ni adhabu, na anayo kubashirieni kwayo, nayo ni thawabu baada ya kufufuliwa, na kukusanywa, na kuhisabiwa, yatakuja tu hapana hivi wala hivi. Wala nyinyi hamwezi kumshinda huyo anaye kutakeni Siku hiyo. Basi hamna uwezo wa kukataa kukusanyika wala kuhisabiwa.

jua nani atakuwa na makaazi mema mwishoni. Hakika madhaalimu hawatafanikiwa.¹³⁵

136. Na wamemwekea sehemu Mwenyezi Mungu katika mimea na wanyama alio umba, nao husema: Hii ni sehemu ya Mwenyezi Mungu - kwa madai yao - na hii ni ya miungu tunao washirikisha. Basi vile walivyo wokusudia miungu yao havimfikii Mwenyezi Mungu, na vilivyo kuwa vya Mwenyezi Mungu huwafikia miungu yao. Ni uovu kabisa hayo wanayo yahukumu.¹³⁶

137. Na kadhaalika hao washirika wao wamewapambia wengi katika washirikina kuwauwa watoto wao ili kuwaangamiza na kuwavurugia dini yao. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli penda wasinge fanya hayo. Basi waache na hayo wanayo yazua.¹³⁷

138. Nao husema: Wanyama hawa na mimea hii ni mwiko. Hawatokula ila wale tuwapendao - kwa madai yao tu. Na wanyama hawa imeharimishwa migongo yao kupandwa. Na wanyama wengine hawalitaji jina la Mwenyezi Mungu juu yao. Wanamzulia uwongo tu Mwenyezi Mungu. Atawalipa kwa hayo wanayo mzulia.¹³⁸

139. Na husema: Waliomo matumboni mwa wanyama hawa ni kwa ajili ya wanaume wetu tu, na wameharimishwa kwa wake zetu. Lakini ikiwa nyamafu basi wanashirikiana. Mwenyezi Mungu atawalipa kwa maelezo yao hayo. Hakika Yeye ni Mwenye hikima, Mwenye kujua.¹³⁹

135 Ewe Nabii! Waambie kwa kuwatisha: Fanyeni kama mpendavyo kwa ukomo wa uwezo wenu. Na mimi nitafanya kwa mujibu wa Haki. Na mwishoe bila ya shaka mtajua nani atakuwa na khatima njema katika makaazi ya Akhera. Na hayo watayapata watu wa Haki, hapana hivi wala hivi. Kwa sababu nyinyi ni madhaalimu, na Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuwaandikia kufuzu walio dhulumu.

136 Na washirikina, ambao wanayaabudu masanamu, wamo katika udanganyifu wa daima. Wao hufanya katika aliyi yaumba Mwenyezi Mungu Mtukufu, katika mazao ya mimea, na ngamia, na ng'ombe, na kondoo, fungu la Mwenyezi Mungu Mtukufu wakiwatumilia wageni na wenye haja, na fungu jingine hulitumia katika kuwakhudumia masanamu ambayo wameyafanya ni washirika wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa mujibu wa madai yao! Ama walicho wawekea masanamu huwafikia masanamu yao, na hukitumia kwa ajili yao. Na walicho muwekea Mwenyezi Mungu Mtukufu hakifikii chochote kwa hao wageni na mafakiri! Uovu ulioje huu wa hukumu yao ya dhulma! Kwani wao wameyafanya masanamu ndio wenziwe Mwenye kuumba hiyo mimea na wanyama, na hawatunii inavyo stahiki hicho walicho mwekea Mwenyezi Mungu.

137 Kama ilivyo kuwa hayo mawazo yao yalivyo wapambia huo mgawanyo wa dhulma katika mazao ya mimea, na ngamia, na ng'ombe, na kondoo, alio umba Mwenyezi Mungu, basi kadhaalika mawazo yao yamewapambia, kutokana na hayo masanamu ambayo wanadai kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu, kuwauwa watoto wao pale wanapo zaliwa, na kuwa ati waliweka nadhiri kwa miungu yao kuwachinja watoto wao! Na hakika hayo mawazo yao yanawaangamiza na yanawavurugia mambo ya dini, kwa hivyo hawaielewi vilivyo! Na ilivyo kuwa mawazo yao yamezisaliti akili zao hadi hiyo, basi wewe waachilie mbali wao na hayo wanayo mzulia Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kukuzulia wewe. Nao watakuja pata malipo ya huo uzushi wao. Na hayo ndio matakwa ya Mwenyezi Mungu, kwani angeli taka wasingeli fanya hayo.

138 Na katika mawazo yao ni kusema kwao: Ngamia hawa, na ng'ombe hawa, na mbuzi na kondoo hawa, na mazao haya ya mimea, ni marfuku. Hayali mtu ila wamtakaye katika utumishi wa masanamu. Hayo ni kwa madai yao ya uwongo, wala hayatokani na Mwenyezi Mungu. Na pia husema: Ngamia hawa wameharimishwa migongo yao, basi hapana ruhusa mtu kuwapanda. Nao juu ya hao hawalitaji jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu wanapo wachinja hao ngamia, na ng'ombe, na mbuzi na kondoo. Na hayo ni kwa kule kumzulia uwongo Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ushirikina wao. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu atawalipa adhabu huko Akhera kwa sababu ya uzushi wao, na kuharimisha kwao vitu ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuharimisha.

139 Na katika mawazo yao ya uwongo hawa washirikina ni kuwa wanasema: Viliomo matumboni mwa wanyama walio watenga, walio zuwiwa wasichinjwe wala wasipandwe - viliomo matumboni mwao,

140. Hakika wamekhasirika wale ambao wamewauwa watoto wao kwa upumbavu pasipo kujua, na wakaharimisha alivyo waruzuku Mwenyezi Mungu kwa kumzulia Mwenyezi Mungu. Hakika wamepotea, wala hawakuwa wenye kuongoka.¹⁴⁰

141. Na Yeye ndiye aliye ziumba bustani zenye kutambaa juu ya chanja, na zisio tambaa, na mitende, na mimea yenye matunda mbali mbali, na mizaituni na mikomamanga inayo fanana na isiyo fanana. Kuleni matunda yake inapo zaa, na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake. Wala msitumie kwa fujo. Hakika Yeye hawapendi watumiayo kwa fujo.¹⁴¹

142. Na katika wanyama amekujaalieni wenye kubeba mizigo na kutoa matandiko. Kuleni katika alivyo kuruzukuni Mwenyezi Mungu, wala msifuuate nyayo za Shet'ani. Hakika yeye ni adui yenu dhaahiri.¹⁴²

143. Amekuumbieni namna nane za wanyama: Wawili katika kondoo, na wawili katika mbuzi. Sema je, ameharimisha yote madume wawili au majike wawili, au waliomo matumboni mwa majike yote mawili? Niambieni kwa ilimu ikiwa nyinyi mnasema kweli.¹⁴³

144. Na wawili katika ngamia, na wawili katika ng'ombe. Sema: Je, ameharimisha yote madume wawili au majike wawili, au waliomo matumboni mwa yote majike? Au, nyinyi mlikuwapo Mwenyezi Mungu alipo kuusieni haya? Basi ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule aliye mzulia Mwenyezi Mungu uwongo, kwa ajili ya kuwapoteza

yaani watoto, wanafaa kuliwa na wanaume, na haramu kwa wanawake. Na juu ya hivyo akizaliwa naye kesho kufa wote wanashirikiana wanakula! Mwenyezi Mungu Mtukufu atawalipa kwa uwongo wao walio mzulia kwa kitendo chao. Kwani wanadai kuwa kuharimishwa huku kunatokana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na hakika Mwenyezi Mungu anajua kila kitu, na ni Mwenye hikima. Vitendo vyake vyote ni kwa mujibu wa hikima. Naye atawalipa wenye dhambi kwa dhambi zao.

140 Hakika wamekhasiri hao walio wauwa watoto wao kwa ujinga na kwa mawazo ya uwongo, bila ya kujua nini matokeo ya kitendo chao, wala sababu yake; na wakajiharimishia nafsi zao riziki alizo waruzuku Mwenyezi Mungu katika mimea, na wanyama, huku wakimzulia Mwenyezi Mungu kwa kudai kuwa ni Yeye ndiye aliye harimisha. Na hakika wamejitenga mbali na Haki kwa sababu hiyo. Na kwa sababu ya uzushi huu hawakuwa katika wanao sifika kwa uwongofu.

141 Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye umba bustani za matunda. Ipo miti inayo pandwa na kuegemezwa juu ya chanja, na ipo isiyo hitajia chanja. Na ameumba mitende, na mimea mingine inayo toa matunda yanayo kihalifiana kwa rangi, na utamu, na sura, na harufu na mengineyo. Na ameumba mizaituni, na makomamanga (makudhumani), yenye kushabihiana katika baadhi ya sifa zake, na isiyo shabihiana, ijapo kuwa udongo huenda ukawa ule ule, na yote ikawa inanyweshwa na maji yale yale. Basi kuleni matunda yake mkipenda, na toeni sadaka yake yanapo wiva na kuyachuma. Wala msifanye fujo katika kula, mkajidhuru wenyewe, na mkawadhuru mafakiri katika kuwanyima haki yao. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi watumiao kwa fujo, katika mwendo wao na vitendo vyao.

142 Na Mwenyezi Mungu ameumba katika nyama hoa, nao ni ngamia, na ng'ombe, na kondoo, na mbuzi, wale wanao beba mizigo yenu, na wale ambao katika sufi yao na manyoya yao na nyewelee zao mnatoa matandiko. Na hiyo ni riziki aliyo kujaalieni Mwenyezi Mungu. Basi kuleni alichu kuhalalishieni Mwenyezi Mungu, wala msimfuuate Shetani na marafiki zake katika kuzua vya halali na haramu, kama walivyo kuwa wakifanya watu wa Jahiliya! Hakika Shetani hakutakiini kheri, kwa sababu yeye ni adui yenu, mwenye uadui dhaahiri.

143 Mwenyezi Mungu ameumba katika kila namna ya nyama hoa dume na jike. Hizo basi ni namna nane. Kondoo namna mbili, mbuzi namna mbili. (ngamia na ng'ombe wametajwa katika Aya inayo fuata.) Ewe Muhammad! Waambie washirikina kukanya hayo waliyo yaharimisha: Nini sababu ya kuharimisha katika hawa kama mnavyo dai? Ni kwa kuwa madume? Au kwa kuwa ni kuwa matumboni ya mama zao? Hayo hayawezi kuwa hivyo, kwa sababu nyinyi hamkuharimisha watoto waliomo tumboni kabisa!! Nambieni kwa mategemeo baraabara, ikiwa nyinyi mnasema kweli katika kuhalalisha na kuharimisha.

watu bila ya ilimu? Hakika Mwenyezi Mungu hawahidi watu madhaalimu.¹⁴⁴

145. Sema: Sioni katika yale niliyo funuliwa mimi kitu kilicho harimishwa kwa mlaji kukila isipo kuwa kiwe ni nyamafu, au damu inayo mwagika, au nyama ya nguruwe, kwani hiyo ni uchafu; au kwa upotofu kimechinjwa kwa jina la asiye kuwa Mwenyezi Mungu. Lakini mwenye kushikwa na dharura, bila ya kutamani wala kupita mipaka, basi hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.¹⁴⁵

146. Na wale walio fuata dini ya Kiyahudi tumewaharimishia kila mwenye kucha. Na katika ng'ombe na kondoo na mbuzi tumewaharimishia shahamu yao, isipo kuwa ile iliyo beba migongo yao au matumbo yao, au iliyo gandamana na mifupa. Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao. Na bila ya shaka Sisi ndio wasema kweli.¹⁴⁶

147. Wakikukanusha basi wewe sema: Mola Mlezi wenu ni Mwenye rehema iliyo enea. Wala haizuiliki adhabu yake kwa watu wakhalifu.¹⁴⁷

148. Watasema walio shirikisha: Lau kuwa Mwenyezi Mungu ange taka tusingeli shiriki sisi, wala baba zetu; wala tusingeli harimisha kitu chochote. Vivi hivi walikanusha walio kuwa kabla yao mpaka walipo onja adhabu yetu. Sema: Je, nyinyi mnayo ilimu mtutolee? Nyinyi hamfuati ila dhana. Wala hamsemi ila uwongo tu.¹⁴⁸

144 Na Mwenyezi Mungu ameumba ngamia namna mbili, dume na jike, na ng'ombe namna mbili mbili vile vile. Ewe Muhammad! Waambie kwa kuwakanya: Nini sababu ya kuwaharimisha hao mlio harimisha kama mnavyo dai? Ni kwa kuwa wao ni madume? Sivyo hivyo; kwa sababu pengine mnahalalisha madume! Au ni kwa kuwa majike? Pia sio hivyo, kwa sababu mnahalalisha majike wakati mwingine! Au kwa kuwa wana watoto matumboni mwao? Pia sio hivyo, kwa sababu hamkuharimisha watoto walio matumboni daima. Nanyi mnadai kuwa kuharimisha huku kunatokana na Mwenyezi Mungu! Nyinyi mlikuwapo Mwenyezi Mungu alipo kuharimisheni haya na mkamsikia makatazo yake? Kabisa hayo hayakuwa. Wacheni mlio nayo; kwani hiyo ni dhulma. Na hapana mwenye kudhulumu zaidi kuliko mwenye kumzulia uwongo Mwenyezi Mungu, akamnasibisha nayo mambo yasiyo toka kwake, wala hayana tegemeo lolote la ki-ilimu la kutegemea, bali huyo anataka kuwapotosha watu tu! Mwenyezi Mungu hawawafikishi wenye kudhulumu wakikhiari njia ya upotovu.

145 Ewe Nabii! Sema: Hivi sasa sipati katika panapo toka mambo ya kuhalalisha na kuharimisha katika niliyo funuliwa mimi wahyi juu ya chakula kilicho harimishwa kula mlaji, isipo kuwa kitu hicho kiwe ni nyamafu, kimekufa na hakikuchinjwa kwa njia za sharia; au damu inayo tiririka, au nyama ya nguruwe - kwani hivyo vilivyo tajwa vinadhuru, na vichafu, havijuzu kula. Na pia katika vitu vilivyo harimishwa kula vinavyo toka katika itikadi sahihi, kwa kuwa wakati wa kuchinjwa lilitajwa jina lisilo kuwa la Mwenyezi Mungu, kama sanamu au muabudiwa mwenginewe! Juu ya hivyo mwenye kulazimika kwa dharura kula kitu katika hivi vilivyo harimishwa, bila ya kuwa anatafuta utamu tu wa kula, na bila ya kupita mpaka wa ile dharura, basi huyo hana dhambi. Kwa sababu Mola wako Mlezi ni Mwenye kughufria, na Mwenye kurehemu.

146 Basi hivi ndivyo tulivyo kuharimishieni nyinyi. Na Mayahudi tuliwaharimishia nyama na shahamu na kila kitu cha wenye makucha katika wanyama, kama ngamia na wanyama wawindao. Na katika ng'ombe na mbuzi na kondoo tuliwaharimishia shahamu yake tu, ila shahamu ya mgongoni, au iliyoko matumboni, au iliyo changanyika na mafupa. Na kuharimishwa huku kulikuwa kwa ajili ya kuwatesa tu kwa ajili ya dhulma zao, na kuziachisha nafsi zao waweze kujilinda na matamano. Na hakika Sisi tunasema kweli katika maneno yetu yote, na miongoni ya hayo ni khabari hii.

147 Wakanushi wakikukanusha katika haya tuliyo kuletea wahyi, waambie kwa kuwahadharisha: Hakika Mola Mlezi wenu, ambaye anapasa mumuamini Yeye peke yake, na mfuate hukumu zake, ana rehema iliyo enea na kumfikia kila anaye mt'ii, na pia anaye muasi kwa kuwa hafanyi haraka kuwaadhibu. Na lakini haitakikani mghurike na hivyo kuwa rehema yake imeenea kote, kwa sababu adhabu yake haina budi kuwafikia hao wakhalifu.

148 Kwa kutaka kujitolea udhuru kwa ushiriki wao, na kule kuharimisha vyakula alivyo halalisha Mwenyezi Mungu, na kukanusha yaliyo wafikia kuwa Mwenyezi Mungu kaudhika nao kwa vitendo vyao, washirikina watasema: Ushirikina wetu na kuharimisha alichu halalisha Mwenyezi Mungu, ni kwa mujibu wa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kuridhi kwake! Na lau angeli penda Yeye kinyume cha hayo,

149. Sema: Basi Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye hoja ya kukata. Na kama angeli penda angeli kuhidini nyote.¹⁴⁹

150. Sema: Leteni mashahidi wenu watao shuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ameharimisha hawa. Basi wakishuhudia, wewe usishuhudie pamoja nao. Wala usifuate matamano ya walio zikanusha Ishara zetu, wala hawaiamini Akhera, na ambao wanamlinganisha Mola Mlezi wao na wengine.¹⁵⁰

151. Sema: Njooi nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi tunakuruzukuni nyinyi na wao. Wala msikaribie mambo machafu, yanayo onekana, na yanayo fichikana. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini.¹⁵¹

152. Wala msiyakaribie mali ya yatima ila kwa njia ya wema kabisa, mpaka afikilie utu-uzima. Na timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu. Sisi hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Na msemapo semeni kwa uadilifu ingawa ni jamaa. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni. Hayo amekuusieni ili mpate kukumbuka.¹⁵²

na angeli chukia tuyatendayo, basi tusingeli mshirikisha sisi wala walio tutangulia, na wala tusingeli harimisha kitu chochote alichu tuhalalishia. Na walio kabla yao waliwakadhibisha Mitume wao, kama hawa wanavyo kukadhibisha wewe. Na waliendelea katika kukanusha kwao mpaka ikawafikia adhabu yetu! Waambie hawa wanao kanusha: Jee mnao ushahidi wa kutegemea ulio sahihi ya kwamba Mwenyezi Mungu amekuridhieni nyinyi mumshirikishe na mhalalishie, mkatutolea? Katika maneno yenu hamfuati ila kudhania tu. Na hiyo haitoshelezi chochote katika Haki. Na nyinyi si chochote, si lolote, ila ni waongo tu katika hayo mnao dai.

149 Ewe Nabii! Sema: Mwenyezi Mungu ana hoja iliyo wazi kuwa nyinyi ni waongo katika madaai yenu kuwa Mwenyezi Mungu ameridhia vitendo vyenu! Wala hamna hoja katika ushirikina wenu, na kuhalalisha kwenu, na kuharimisha kwenu, na mengineyo. Na Mwenyezi Mungu angeli taka mhidike angeli kuhidini nyote mkafuata Njia ya Haki. Lakini hakutaka hayo kwa kuwa nyinyi mmekhiari njia ya upotovu.

150 Ewe Nabii! Waambie: Leteni wasaidizi wenu watao kushuhudieni kwamba kweli Mwenyezi Mungu ameharimisha hivi mnavyo dai kuwa ni haramu. Wakihudhuria na wakashuhudia, basi wewe usiwasadiki, kwa sababu hao ni waongo. Wala usifuate matamano ya hawa walio kanusha hoja za uumbaji na Qur'ani inayo somwa, na ambao hawaiamini Akhera nao wanamshirikisha Mwenyezi Mungu, wanamfanya Yeye sawa na hao miungu inayo abudiwa kwa uwongo.

151 Ewe Nabii! Waambie: Njooi nikubainishieni yaliyo haramu ambayo inatakana mshughulike nayo, na mjitenge nayo. Msimfanye yeyote kuwa ni mshirika na Mwenyezi Mungu, kwa shirki ya namna yoyote. Wala msiwafanye uovu wazazi wenu, bali wafanyieni wema mwisho wa wema. Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya kukufikieni ufakiri, au mnao ogopa usikufikieni siku za usoni. Kwani nyinyi sio mnao toa riziki. Bali Sisi ndio tunakuruzukuni nyinyi na tunawaruzuku wao. Wala msikaribie uchafu wa uzinzi, kwani huo ni katika mambo mabaya yanayo katazwa, sawa sawa ikiwa jahara au kwa siri asiyo iona ila Mwenyezi Mungu. Wala msiuwe nafsi yoyote aliyo kataza Mwenyezi Mungu kuiuwa kwa kutokuwapo kupasa kwake, ila ikiwa kuuwa huko ni kwa haki ya kutekeleza hukumu ya mahkama. Mwenyezi Mungu amekuamrishiwa kwa amri ya nguvu muepuke haya yaliyo katazwa ambayo akili ya maumbile inakwambieni mupekane nayo, ili nanyi myatie akilini hayo.

152 Wala msiyatumie mali ya yatima ila kwa njia iliyo bora kabisa ya kuyahifadhi na kuyakuza. Na endeeleni hivyo mpaka huyo yatima afike umri wa uwongofu, atapo weza mwenyewe kuendesha mambo yake baraabara. Hapo tena ndio mpeni mali yake. Wala msipunje vipimo na mizani kwa kupunguza mnapo toa, au kuongeza mnapo chukua. Bali pimeni kwa uadilifu kama muwezavyo. Na Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi ila kwa kadiri iwezavyo bila ya karaha. Na mkisema neno katika kuhukumu, au ushahidi, au khabari, au mfano wa hayo, basi msikengeuke mkaacha uadilifu na ukweli. Bali hakikisheni kusema sawa, bila ya kuzingatia makhusiano ya jinsi, yaani uke na ume, au rangi, au ujamaa au ushemeji. Wala msitenge ahadi za Mwenyezi Mungu alizo chukua kwenu kwa taklifu, wala ahadi zililo baina

153. Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuatene njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuchamngu.¹⁵³

154. Tena tulimpa Musa Kitabu kwa kumtimizia (neema) aliye fanya wema, na kuwa ni maelezo ya kila kitu, na uwongofu na rehema, ili wapate kuamini mkutano wao na Mola wao Mlezi.¹⁵⁴

155. Na hichi ni Kitabu tulicho kiteremsha, kilicho barikiwa. Basi kifuateni, na mchenimngu, ili mrehemewe.¹⁵⁵

156. Msije mkasema: Hakika mataifa mawili kabla yetu yameteremshiwa Kitabu; na sisi tulikuwa hatuna khabari ya waliyo kuwa wakiyasoma.¹⁵⁶

157. Au mkasema: Lau kuwa tumeteremshiwa sisi Kitabu tungeli kuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu, na rehema. Basi nani aliye dhaalimu mkubwa zaidi kuliko yule anaye kanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, na akajitenga nazo? Tutawalipa wanao jitenga na Ishara zetu adhabu kali kabisa kwa sababu ya kujitenga kwao.¹⁵⁷

158. Wanangoja jengine ila wawafikie Malaika, au awafikie Mola wako Mlezi, au zifike baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi? Siku zitakapo fika baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi, kuamini hapo hakutumfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake, au amefanya kheri katika Imani yake. Sema: Ngojeni, nasi pia tunangoja.¹⁵⁸

yenu wenyewe kwa wenyewe, katika mambo yaliyo fungamana na maslaha yaliyo ruhusywa kisharia. Bali timizeni ahadi hizi zote. Mwenyezi Mungu amekuamrisheni kwa kutilia mkazo mjitenge na yaliyo katazwa, na mkumbuke kuwa Sharia ni kwa ajili ya maslaha yenu.

153 Wala msiiache Njia niliyo kuwekeeni, kwani hiyo ndiyo Njia Iliyo Nyooka itayo kufikisheni kwenye mafanikio ya duniani na Akhera. Bali ifuateni Njia hii, wala msifuatene njia nyingine za upotovu alizo kukatazeni Mwenyezi Mungu, ili msije kufarikiana mkawa makundi na mapande mapande, ya madhehebu na vyama, na mkawa mbali na Njia ya Mwenyezi Mungu iliyo kaa sawa. Mwenyezi Mungu amekuamrisheni kwa amri ya nguvu ili msije mkamkhalifu Yeye.

154 Na tulimteremshia Musa Taurati kwa kumtimizia neema mtu aliye simama msimamo mwema katika mambo ya Dini. Na tuliiteremsha kwa kueleza wazi kila jambo katika mafunzo yalio nasibiana na watu wake, na ni uwongofu kwenda Njia iliyo sawa, na rehema kwao kwa kuifuata. Na hayo ni hivyo ili Wana wa Israili waiamini Siku ya kukutana na Mola wao Mlezi, Siku ya Kiyama na kuhisabiwa kwa mambo walio amrishawa kuyafanya.

155 Na hii Qur'ani ni Kitabu, kilicho barikiwa, tulicho kiteremsha, chenye kukusanya kheri za Mwenyezi Mungu, na manufaa ya Dini na dunia. Basi kifuateni, na ogopeni msende kinyume chake, ili Mola wenu Mlezi apate kukurehemuni.

156 Tumeiteremsha hii Qur'ani ili msipate kutoa udhuru kwa uasi wenu mkasema: Wahyi haukuteremka ila kwa mataifa mawili tu ya kabla yetu, nao ni watu wa Taurati na watu wa Injili. Na sisi hatuna ilimu kabisa ya kusoma vitabu vyao na kufahamu uwongozi uliomo humo.

157 Na Sisi tumeiteremsha Qur'ani ili wasiseme pia: Lau kuwa sisi tumeteremshiwa ufunuo kama walivyo teremshiwa wao, tungeli washinda kwa uwongofu, na hali yetu ingeli kuwa bora zaidi, kwa sababu ya akili zetu ni pana zaidi na sisi tumetengenea vizuri! Baada ya hii leo hamna hoja ya kuasi kwenu. Wala hapana udhuru wa kauli yenu hii. Kwani Qur'ani imekujieni kutoka kwa Mola Mlezi wenu, nayo ni alama iliyo wazi ya ukweli wa Muhammad. Inabainisha yote mnao yahitajia katika Dini yenu na dunia yenu. Inakuongoeni kwenye Njia iliyo sawa, na rehema kwenu kuifuata. Na hapana mwenye kudhulumu zaidi kuliko huyo anaye zikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu alizo ziteremsha katika Vitabu vyake, na Ishara zake alizo ziamba katika ulimwengu, naye akazipuza na asiziamini, na wala asizitende! Na Sisi tutawaadhibu hao wanao zikataa Ishara zetu, wala hawazingatii adhabu yenye mwisho wa uchungu, kwa sababu ya kukataa kwao na kuacha kuzingatia kwao.

158 Hoja imekwisha simama ya kuwa kuamini ni wajibu. Na watu hawa hawakuamini. Basi wanangojea nini ndio waamini? Je, wanangojea wawajie Malaika wawe ni Mitume badala ya kuwa wanaadamu, au wawe ni mashahidi kushuhudia ukweli wako? Au aje Mwenyewe Mola wako Mlezi, wamwone, au

159. Hakika walio igawa Dini yao na wakawa makundi makundi, huna ukhusiano nao wowote. Bila ya shaka shauri yao iko kwa Mwenyezi Mungu; kisha atawaambia yale waliyo kuwa wakiyatenda.¹⁵⁹

160. Afanyae wema atalipwa mfano wake mara kumi. na afanyae ubaya hatalipwa ila sawa nao tu. Na wao hawatadhulumiwa.¹⁶⁰

161. Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Mlezi ameniongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka, Dini iliyo sawa kabisa, ambayo ndiyo mila ya Ibrahim aliye kuwa mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.¹⁶¹

162. Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.¹⁶²

163. Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyo amrisha, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.¹⁶³

164. Sema: Je nitafute Mola Mlezi asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ndiye Mola Mlezi wa kila kitu? Na kila nafsi haichumii ila nafsi yake. Na habebi mwenye kubeba mzigo wa mwenziwe. Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu Mlezi, naye atakuambieni mliyo kuwa mkikhitalifiana.¹⁶⁴

165. Naye ndiye aliye kufanyeni makhalifa wa duniani, na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa, ili akujaribuni kwa hayo aliyo kupeni. Hakika

ashuhudie ukweli wako? Au zije baadhi ya alama za Mola wako Mlezi zishuhudie ukweli wako? Na pindi zikija hizo alama za Mola wako Mlezi za kuwapelekea kuamini, basi Imani yao haitowafaa kitu. Kwani hiyo itakuwa ni Imani ya kahari, hawana hila. Na sasa tena haimfalii mwenye kuasi toba yake na ut'iifu wake. Kiwango cha kufanya waajibu kimekwisha pita! Waambie hawa wanao kataa na kukanusha: Ngojeni moja ya mambo hayo matatu, nanyi endeleeni katika kukanusha kwenu. Nasi pia tunangoja hukumu ya Mwenyezi Mungu juu yenu.

159 Hakika walio igawanya Dini moja ya Haki kwa itikadi za uwongo, na sharia za upotovu, na wakawa kwa sababu hiyo makundi mbali mbali; unawadhania ni wamoja, kumbe nyoyo zao zimekhitalifiana, wewe huna jukumu kwa kufarikiana kwao na uasi wao, wala wewe huwezi kuwahidi. Wewe hulazimiki ila kufikisha Ujumbe. Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kumiliki mambo yao kwa kuwaongoa na kuwalipa, kisha awatajie Siku ya Kiyama yale waliyo kuwa wakiyafanya duniani na awalipe kwayo.

160 Mwenye kutenda mema atalipwa thawabu zake mpaka mara kumi kwa kufadhiliwa na kukirimiwa. Na mwenye kutenda ovu hatoadhibiwa ila kwa kadri ya maasi yake tu, kwa uadilifu wake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na hapo hapana dhulma kwa kumpunguzia mtu thawabu, wala kumzidishia adhabu.

161 Sema ewe Nabii kwa kubainisha Dini ya Haki unayo ifuata: Hakika Mola wangu ameniongoza, na ameniwaifikisha kuishika Njia Iliyo Nyooka, yenye kufika ukomo wa kukamilika na kunyooka. Na Dini hii ndiyo aliyo ifuata Ibrahim akaacha itikadi zote potovu. Na Ibrahim hakuwa akimuabudu mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu, kama wanavyo dai washirikina

162 Sema: Hakika Sala yangu na ibada zangu, na niyafanyayo katika hali ya uhai wangu, nayo ni ut'iifu, na Imani na vitendo vyema ninavyo kufa navyo, vyote hivyo nimevisafia kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu Aliye umba vitu vyote, na kwa hivyo akastahiki kuabudiwa Yeye peke yake, na kut'iwa Yeye peke yake.

163 Hana mshirika katika kumba, wala katika kustahiki kuabudiwa. Naye Yeye Mola Mlezi wangu ameniamrisha kwa hayo nimfanyie ikhlasi (usafi wa niya) katika Tawhidi (kutakasisha upweke wake) na vitendo. Na mimi ni wa kwanza wa kumnyenyekea, kumfuata, na mkamilifu wao wa ut'iifu na kusilimu.

164 . Sema ewe Muhammad, kuwakatalia washirikina wito wao kwako, uwakubalie ushirikina wao: Nitafute wa kumuabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ndiye Muumba wa kila kitu? Na waambie kuwakatalia kuwa wao hawawezi kukubebea makosa yako ikiwa utawakubalia: Hapana nafsi inayo tenda kitu ila itapata malipo yake wenyewe peke yake. Hachukui mtu dhambi za mwenziwe. Kisha mtafululiwa kwa Mola Mlezi wenu baada ya mauti, naye atakupeni khabari ya hayo mliyo khitalifiana kwayo duniani, katika mambo ya itikadi, na atakulipeni kwayo. Basi vipi nimuasi Mwenyezi Mungu kwa kutegemea ahadi yenu ya uwongo.

Sura 6 - Al-An'am

Mola Mlezi wako ni Mwepesi wa kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.¹⁶⁵

165 Na Yeye Mwenyezi Mungu ndiye aliye kufanyeni makhalifa (walio chukua pahala pa) kaumu zilizo tangulia katika kuamirisha ulimwengu. Naye amewanyanyua baadhi yenu kuliko wengine kwa daraja nyingi katika mambo yanayo onekana na yasiyo onekana kwa vile kukupeni njia za kuyafikilia, ili apate kukujaribuni, kukufanyieni mtihani, katika hizo neema alizo kupeni, vipi mtazishukuru, na katika sharia alizo kupeni mtazitumia vipi. Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwepesi wa kuwaadhibu wakhalifu, kwani hakika adhabu yake itakuja tu bila ya shaka, na kila lijalo lipo karibu. Na Yeye ni mwenye maghfira makubwa kwa makosa ya wenye kutubu na wakatengenea, na Mkunjufu wa rehema kwao.

Sura 7 - Al-A'raaf

Utangulizi

Sura hii imeteremka Makka isipo kuwa Aya nane, nazo ni 163 mpaka 170. Na idadi za Aya zake ni 206.

Mwanzo wa Sura hii ni kuendeleza yaliyo kuja mwisho wa Sura ya Al-Ana'm, na baada ya hayo imeingia kueleza khulka ya kibinaadamu. Ikataja kisa cha Adam na Hawa, na walivyo toka kwenye Bustani kwa kutiwa wasiwasi na Shet'ani, na ikaeleza huo wasiwasi unaoendelea kwa watu katika mavazi na chakula. Kisha Aya za Sura hii tukufu, kama sura nyengine za Qur'ani zikaingia kutupia jicho kwenye mbingu na ardhi na viliomo ndani yao, na kuzingatia uumbaji wake wa ajabu.

Kadhaalika Sura hii imeeleza hadithi za Manabii kama Nuhu na Hud na kaumu yake kina A'ad. Kisha hadithi ya Saleh na kaumu yake, Thamud, walio sifika kwa nguvu zao na wakapewa utajiri; na hadithi ya Lut' na kaumu yake, na ikataja maovu waliyo kuwa wakiyafanya; na hadithi ya Shua'ib na watu wa Madyana. Na baada ya hadithi hizo za kweli Sura imeeleza mafunzo na mazingatio yaliyomo. Naye *Subhanahu wa Ta'ala* amefuatilizia hayo kwa kisa cha Musa na yaliyo tokea katika mambo ya Firauni.

Na Sura ikakhitimishia kwa kumathilisha nini hali ya mwenye kupewa hidaya khalafu akabanduka kwenye uwongofu akaingia kwenye upotovu kwa kumfwata Shet'ani, na Sura pia ikamalizia kueleza Wito wa kuendea Haki alio kuja nao Muhammad, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

1. ALIF LAM MYM 'SAAD'

2. Kitabu kilicho teremshwa kwako - basi isiwe dhiki kifuani kwako kwa ajili yake, upate kuonya kwacho, na kiwe ni ukumbusho kwa Waumini.²

3. Fuateni mliyo teremshiwa kutoka kwa Mola Mlezi wenu, wala msifuate rafiki au walinzi wengine badala yake. Ni machache mnayo yakumbuka.³

4. Na miji mingapi tuliangamiza, ikaifikia adhabu yetu usiku au walipo kuwa

1 Alif Lam Mym 'Saad. (A.L.M.S'.) Hizi ni harufi za kutamkwa ambazo zinaanzia baadhi ya Sura za Makka, kwa ajili ya kuwazindua Washirikina kuwa hakika hii Qur'ani Tukufu imeundwa kwa harufi zile zile wanazo zitamka wao. Na juu ya hivyo wao wanaemewa hawawezi kuleta mfano wake. Kadhaalika harufi hizi zinapo somwa huwazindua wao wasikilize, kwa kuwa walikuwa wananasihiwa na wakubwa zao kuwa wasisikilize Qur'ani.

2 (Ewe Nabii!) Umeteremshiwa wewe Qur'ani ili uwaonye hao wanao kanya wapate kuamini, na uwakumbushe Waumini wapate kuzidi Imani yao. Basi usiingie dhiki katika kifua chako unapo ifikilisha kwa kukhofu kuwa utakanushwa.

3 (Enyi Watu!) Fuateni aliyu kufunulienu Mola wenu Mlezi, wala msiwafuate marafiki au walinzi wengineo badala yake Yeye, mkawa mnawaitikia wao na mkiwaomba msaada! Itakuwa kama hamkuwaidhika ikiwa mtaicha Dini ya Mwenyezi Mungu na muifuate nyengineyo, hali ya kuwa yapo mengi ya kuzingatia katika haya mliyo funuliwa.

wamelalaadhuhuri.⁴

5. Basi hakikuwa kilio chao ilipo wafikia adhabu yetu, isipo kuwa kusema: Hakika sisi tulikuwa wenye kudhulumu.⁵

6. Na kwa yakini tutawauliza wale walio pelekewa Ujumbe, na pia tutawauliza hao Wajumbe.⁶

7. Tena tutawasimulia kwa ilimu; wala Sisi hatukuwa mbali.⁷

8. Na Siku hiyo kipimo kitakuwa kwa Haki. Basi watakao kuwa na uzani mzito, hao ndio watakao fanikiwa.⁸

9. Na watakao kuwa na uzani khafifu, basi hao ndio walio zitia khasarani nafsi zao kwa sababu ya kuzipinga Ishara zetu.⁹

10. Na hakika tumekuwekeni katika ardhi, na tumekujaalieni humo njia za kupatia maisha. Ni kuchache kushukuru kwenu.¹⁰

11. Na hakika tulikuumbeni, kisha tukakutieni sura, kisha tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam. Basi wakasujudu isipo kuwa Iblisi, hakuwa miongoni mwa walio sujudu.¹¹

12. Mwenyezi Mungu akasema: Nini kilicho kuzuia kumsujudia nilipo kuamrisha? Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, naye umemuumba kwa udongo.¹²

13. Akasema: Basi teremka kutoka humo! Haikufalii kufanya kiburi humo. Basi toka!

4 Kwani Sisi tumekwisha iteketeza miji kadhaa wa kadhaa, kwa sababu watu wao walikuwa wakiwaabudu wasio kuwa Mwenyezi Mungu, na kwa kuwa katika mwendo wao hawakufuata Njia yake. Ikawajia adhabu yetu wakati wao wameghafilika na wametua usiku nao wamelala, kama yalivyo wapata kaumu ya Lut'; au wakatekezwa mchana nao wamepumzika wakati wa kujinyoosha, kama yalivyo wapata kaumu ya Shua'ib.

5 Basi wakaungama kwa madhambi yao yaliyo waletea msiba wao. Hakuwa hata mmoja katika wao walipo ona adhabu ila alisema, na wakati huo kusema huko hakufai kitu: Hakika sisi tulikuwa tumejidhulumu nafsi zetu kwa maasiya, wala Mwenyezi Mungu hakutudhulumu kwa kutupa adhabu.

6 Na Siku ya Kiyama hisabu ya Mwenyezi Mungu itachungua kila kitu kwa uadilifu. Tutawauliza watu tulio watumia Mitume: Je, Ujumbe umewafikilia? Na wamewajibu nini hao Wajumbe tulio watuma? Na tutawauliza Mitume pia: Je, mmefikisha yaliyo teremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi? Na hao kaumu zenu wamekujibuni nini.

7 Na tutawapa wote khabari ya kweli yote yaliyo kuwa kwao, kwa sababu hakika Sisi tumewadhibitia kila kitu chao, kwani Sisi hatukuwa mbali nao, wala hatukuwa hatujui waliyo kuwa wakiyafanya.

8 Na Siku tutapo wauliza na kuwaeleza, vipimo vya vitendo vyao kwa ajili ya kulipwa vitakuwa vipimo vya uadilifu. Wale ambao mema yao yatazidi kuliko maovu yao watakuwa ndio wenye kufuzu, tutakao walinda na Moto na tutawatia Peponi.

9 Na wale ambao maovu yao yatakithiri kuliko mema yao, hao ndio watakuwa khasarani, kwa kuwa wameziua nafsi zao kwa Shetani, wakaacha kuzingatia Ishara zetu kwa ukafiri na inda.

10 Nasi tumekuwekeni katika ardhi, na tukakupeni nguvu za kuiamirisha mkajipatia manufaa ndani yake, na tukakusahilishieni njia za kupatia maisha. Juu ya neema hizi zote, kumekuwa kuchache mno kumshukuru kwenu Mwenyezi Mungu. Nanyi mtakuja pata malipo ya hayo myatendayo!

11 Na katika khabari za wale wa mwanzo pana mazingatio na mawaidha, yanayo dhahirisha kuwa Shetani anajaribu akuondoleeni neema kwa kusahau kwenu amri za Mwenyezi Mungu. Sisi tumemuumba baba yenu Adam, na tukampa Sura. Kisha tukawaambia Malaika: Mtukuzeni! Wakamtukuza kwa kut'ii amri ya Mola wao Mlezi, ila Iblisi hakut'ii.

12 Mwenyezi Mungu kwa kuudhika naye kwa uasi wake alimwambia: Nini kilicho kuzuia usimtukuze Adam, na hali Mimi nimekuamrisha ufanye hivyo? Iblisi akajibu kwa inda na kiburi: Mimi bora kuliko Adam. Umeniumba kwa moto, na yeye umemuumba kwa udongo. Na moto ni mtukufu zaidi kuliko udongo.

Hakika wewe u miongoni mwa walio duni.¹³

14. Akasema: Nipe muhula mpaka siku watakapo fufuliwa.¹⁴

15. Akasema: Utakuwa miongoni mwa walio pewa muhula.¹⁵

16. Akasema: Kwa kuwa umenihukumia upotofu, basi nitawavizia katika Njia yako Iliyo Nyooka.¹⁶

17. Kisha nitawazukia mbele yao na nyuma yao na kuliani kwao na kushotoni kwao. Wala hutawakuta wengi wao wenye shukrani.¹⁷

18. Akasema: Toka humo, nawe umekwisha fedheheka, umekwisha fukuzwa. Hapana shaka atakaye kufuata miongoni mwao, basi nitaijaza Jahannam kwa nyinyi nyote.¹⁸

19. Na wewe, Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani hii, na kuleni humo mpendapo. Wala msiukaribie mti huu, mkawa katika wale walio dhulumu.¹⁹

20. Basi Shet'ani aliwatia wasiwasi ili kuwafichulia tupu zao walizo fichiwa, na akasema: Mola Mlezi wenu hakukukatazeni mti huu ila msije mkawa Malaika, au msije mkawa katika wanao ishi milele.²⁰

21. Naye akawaapia: Kwa yakini mimi ni miongoni wa wanao kunasihini.²¹

22. Basi akawateka kwa khadaa. Walipo uonja ule mti, tupu zao zilifichuka na wakaingia kujibandika majani ya Bustanini. Mola wao Mlezi akawaita: Je, sikukukatazeni mti huo, na kukwambieni ya kwamba Shet'ani ni adui yenu wa dhaahiri?²²

23. Wakasema: Mola wetu Mlezi! tumejidhulumu nafsi zetu, na kama hutusamehe na kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kukhasirika.²³

24. Akasema: Teremkeni! Mtakuwa nyinyi kwa nyinyi maadui. Na kwenye ardhi

13 Mwenyezi Mungu alimlipa kwa inda yake na kiburi chake kwa kumfukuza katika makao ya utukufu wake, na akamwambia: Teremka kutoka hapo baada ya kuwa katika pahala pa juu. Haikufalii ukapandwa kichwa na ukaasi humo! Toka huko, nawe umehukumiwa hizaya na udhalili!

14 Iblisi akamwambia Mwenyezi Mungu: Nipe muhula, unibakishe mpaka Siku ya Kiyama.

15 Mwenyezi Mungu akamjibu: Wewe utakuwa katika walio bakishwa wa mwisho.

16 Kwa kumchukia Adam na kumhusudu alisema: Kwa sababu ya kunihukumia kupotoka na kupotea, nakuapia nitawapoteza wanao wa Adam wasiifuate Njia yako Iliyo Nyooka, kwa kutumia kila hila zinazo mkinika.

17 Na ninaapa, nitawatokelea mbele yao, na nyuma yao, na kuliani kwao, na kushotoni kwao, na kila upande ninao weza, nikitafuta kila kipengee cha kughafilika kwao au udhaifu wao, nipate kuwapotosha, hata wasiwe wengi wao wanao kuamini Wewe, kwa kuto shukuru neema yako.

18 Mwenyezi Mungu akazidi kuudhika, akamwambia: Toka kwenye makao ya ukarimu wangu, wewe ulio hizika kwa kiburi chako na uasi wako, na khatima yako ni kuhiliki tu! Na ninaapa nitaijaza Jahannamu kwa wewe na hao wanao wa Adam watao kufuata nyote pamoja!

19 Na ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika makao ya ukarimu wangu, nayo ndiyo hiyo Bustani, mneemeke humo, mkila kila chakula mpendacho, isipo kuwa mti huu. Msiukaribie! Msije mkawa wenye kujidhulumu nafsi zenu kwa adhabu itayo kupateni kwa kuvunja amri.

20 Shetani akawazaini waivunje amri ya Mwenyezi Mungu, ziwavuke nguo zilizo wasitiri zikashifike tupu zao. Akawaambia: Mola wenu Mlezi hakukukatazeni mti huu ila ni kwa kuwa hataki muwe Malaika, au msije mkawa mnaishi milele, na neema yenu haikatiki daima katika makao haya.

21 Naye akawaapia kuwa ati yeye ni katika wanao wapa nasaha njema, na akakariri kiapo chake.

22 Basi akawachochea kwa udanganyifu mpaka wakenda kula ule mti. Walipo uonja tupu zao zikafichuka, wakaingia wanakusanya majani ya miti kujisitiri tupu zao. Mola wao Mlezi akawakaripia, na akawatanabahisha makosa yao kwa kuwambia: Mimi sikukukatazeni mti ule, na nikakwambieni kuwa Shetani ni adui yenu wa dhaahiri, hakutakieni kheri?

23 Adam na mkewe wakasema nao wamejuta wananyenyekea: Ewe Mola wetu Mlezi! Tumejidhulumu nafsi zetu kwa kuvunja amri yako, kuliko pelekea kuondoka kwa neema. Na ikiwa hutusamehe ukhalifu wetu, ukaturehemu kwa fadhila yako, hapana shaka tutakuwa katika wenye kukhasiri.

itakuwa ndio makao yenu na starehe yenu mpaka ufike muda.²⁴

25. Akasema: Humo mtaishi, na humo mtakufa, na kutoka humo mtatolewa.²⁵

26. Enyi wanaadamu! Tumekuteremshieni nguo za kuficha tupu zenu, na nguo za pambo. Na nguo za uchamngu ndio bora. Hayo ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu mpate kukumbuka.²⁶

27. Eny wanaadamu! Asije Shet'ani kukufitinini kama alivyo watoa wazazi wenu Peponi, akawavua nguo zao kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye na kabila yake wanakuoneni, na nyinyi hamuwaoni. Hakika Sisi tumewafanya Mashet'ani kuwa ni marafiki wa wasio amini.²⁷

28. Na wanapo fanya mambo machafu husema: Tumewakuta nayo baba zetu, na Mwenyezi Mungu ametuamrisha hayo. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu haamrishi mambo machafu. Mnamzulia Mwenyezi Mungu msiyo yajua?²⁸

29. Sema: Mola Mlezi wangu ameamrisha uadilifu, na mumuelekeze nyuso zenu kila mnapo sujudu, na muombeni Yeye kwa kumsafia Dini. Kama alivyo kuumbeni mwanzo ndivyo mtavyo rudi,²⁹

30. Hali ya kuwa kundi moja amelihidi, na kundi jengine limethibitikiwa na upotofu. Kwa hakika hao waliwafanya mashet'ani kuwa ndio marafiki walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, na wanadhani kuwa wao wameongoka.³⁰

24 Mwenyezi Mungu akawaambia wao na pia na Shetani: Teremkeni nyote nyinyi, mtakuwa maadui nyinyi kwa nyinyi. Makao yenu na starehe yenu kwa muda mpaka ifike ajali yenu, yatakuwa katika ardhi. 25 Katika ardhi mnazaliwa, na mnaishi, na humo mnakufa na kukizwa. Na kutoka huko mtatolewa wakati wa kufufuliwa.

26 Enyi Binaadamu! Sisi tumekunemesheni. Tumekuumbieni nguo kusitiri tupu zenu, na vitu vya pambo. Lakini ut'iifu ndio nguo bora ya kukukingeni na adhabu. Neema hizo ni katika Ishara zenye kuonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu, na rehema yake, ili watu waukumbuke utukufu wake. Yeye tu ndiye anaye stahiki Ungu. Na kisa hichi ni katika nyendo za Mwenyezi Mungu za uumbaji wake, zinazo bainisha nini malipo ya kuvunja amri ya Mwenyezi Mungu, ili watu wakumbuke, na wafanye pupa kumt'ii Allah na kumshukuru.

27 Enyi wanaadamu! Msimuitikie Shetani na upotovu wake, mkatoka kwenye neema hizi, ambazo hazidumu ila kwa kushukuru na kut'ii, kama walivyo mitikia wazazi wenu, Adam na mkewe, akawatoa Shetani kwenye neema na ukarimu, na akawavua nguo zao zikaonekana tupu zao. Basi yeye Shetani na wasaidizi wake wanakujieni kwa namna msio watambua, wala hamuhisi mipango yao na vitimbi vyao! Lakini Shetani hana madaraka juu ya Waumini. Sisi tumemfanya yeye na wasaidizi wake kuwa ni marafiki wa wale wasio amini Imani ya kweli yenye kulazimikana na ut'iifu ulio timia.

28 Na wakanushao wakitenda jambo ovu la mwisho, kama shirki, na kut'ufu kwenye Al Ka'aba nao wako uchi, na mengineyo, basi wao hutoa udhuru kwa kusema: Sisi tumewakuta baba zetu wakenda mwendo huu huu, na sisi tunawafuata wao; na Mwenyezi Mungu ametuamrisha hivi na ameturidhia kwa kuwa ametukiria! Waambie ewe Nabii kuwapinga kwa uzushi wao: Hakika Mwenyezi Mungu hakuamrisha mambo haya maovu! Je, mnamnasibishia Mwenyezi Mungu mambo msiyo kuwa nayo tegemeo lolote mnalo jua lina dalili ya ukweli wa kumnasibisha nalo *Subhanahu*.

29 Wabainishie aliyi yaamrisha Mwenyezi Mungu, useme: Mola Mlezi wangu ameamrisha uadilifu usio ingiliwa na uchafu. Na amekuamrisheni mumkhusishe Yeye tu kwa ibada kila wakati na kila pahala, na muwe wenye kumsafia niya katika hayo. Na nyote nyinyi baada ya kufa ni wenye kurejea kwake. Na kama alivyo anza kukuumbeni kwa wepesi, na mlikuwa hammiliki kitu chochote, basi kadhaalika mtarejea kwake kwa wepesi na hali mmeziacha nyuma ya migongo yenu neema zote mlizo nazo.

30 Siku ya Kiyama watu watakuwa makundi mawili:- Kundi moja lilio pata tawfiqi ya Mwenyezi Mungu kwa kuwa lilichagua Njia ya Haki, likaamini na likatenda vitendo vyema. Na kundi jengine limehukumiwa upotovu, kwa sababu lilikhiari njia ya baat'ili, nayo ni ukafiri na uasi! Na hao walio potea waliwafanya mashetani ndio rafiki zao badala ya Mwenyezi Mungu, wakawafuata, nao wanadhani kuwa wao wamewafikiwa kwa kudanganyika kwao na khadaa za mashetani!

31. Enyi wanaadamu! Chukueni pambo lenu kwenye kila pahala wakati wa ibada, na kuleni, na kunyweni na wala msifanye ubadhirifu. Kwa hakika Yeye hapendi wanao fanya israfu.³¹

32. Sema: Ni nani aliye harimisha pambo la Mwenyezi Mungu alilo watolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki. Sema hivyo ni kwa walio amini katika uhai wa duniani, na Siku ya Kiyama vitakuwa vyao wao tu. Namna hivi tunazieleza Ishara kwa watu wanao jua.³²

33. Sema: Mola Mlezi wangu ameharimisha mambo machafu ya dhaahiri na ya siri, na dhambi, na uasi bila ya haki, na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na asicho kiletea uthibitisho, na kumzulia Mwenyezi Mungu msiyo yajua.³³

34. Na kila umma una muda wake. Utakapo fika muda wao basi hawatakawia hata saa moja, wala hawatatangua.³⁴

35. Enyi wanaadamu! Watakapo kufikieni Mitume miongoni mwenu wakakuelezeni Ishara zangu, basi watakao mchamngu na wakatengenea haitakuwa khofu kwao, wala hawatahuzunika.³⁵

36. Na wale watakao kanusha Ishara zetu na wakazifanyia kiburi, hao ni watu wa Motoni; humo watadumu.³⁶

37. Basi ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye mzulia Mwenyezi Mungu uwongo, au anaye zikanusha Ishara zake? Hao itawafikia sehemu yao waliyo andikiwa, mpaka watakapo wafikia wajumbe wetu kuwafisha, watawaambia: Wako wapi mlio kuwa mkiwaomba badala ya Mwenyezi Mungu? Watasema: Wametupotea!

31 Enyi wanaadamu! Chukueni pambo lenu, nalo ni nguo hizi “maaddiy” za kuonekana, za kusitiri utupu, na nguo za “adabiy” zisizo onekana, bali ni za maana, nazo ni Taqwa, Uchamngu, katika kila pahala pa Sala, na kila wakati mnapo fanya ibada. Na jistarehesheni kwa kula na kunywa bila ya kufanya israfu au ubadhirifu, yaani kutumia kwa fujo, katika hayo. Basi msitumie vitu vilivyo harimishwa, wala msipite kiasi cha kiakili katika huko kujistarehesha. Hakika Mwenyezi Mungu hana radhi na wanao tumia kwa fujo.

32 Ewe Muhammad! Waambie kwa kuupinga ule uzushi wao kumzulia Mwenyezi Mungu juu ya kuhlalisha na kuharimisha: Nani aliye harimisha pambo la Mwenyezi Mungu alilo waambia waja wake? Na nani aliye harimisha riziki iliyo halali na nzuri? Waambie: Hivi vitu vizuri ni neema inayo toka kwa Mwenyezi Mungu. Ingingeli faa wastarehe navyo duniani ila wale walio amini, kwa sababu wao wanatimiza haki yao kwa shukrani na ut’ifu. Lakini rehema ya Mwenyezi Mungu ni kunjufu, imewakusanya pia makafiri na wakhalifu katika dunia. Na Siku ya Kiama neema hizi zitakuwa za Waumini peke yao, wala hapana mwinginewe ataye shirikiana nao katika hayo. Na Sisi tunazieleza Aya, Ishara, zinazo onyesha hukumu kwa mpango huu ulio wazi kwa ajili ya watu wanao fahamu kwamba hakika Mwenyezi Mungu peke yake, Mwenye kumiliki kila kitu, ndiye Mwenye uwezo wa kuhlalisha na kuharimisha.

33 Ewe Muhammad! Sema: Hakika Mola wangu Mlezi ameharimisha mambo yaliyo zidi kwa ubaya, kama uzinzi; sawa sawa ukifanywa kwa siri au kwa dhaahiri. Pia ameharimisha kila maasi ya namna yoyote, na dhulma isiyo na njia ya haki. Na ameharimisha kumshirikisha na chochote kisicho kuwa na hoja madhubuti, au dalili ya kweli. Na pia kumzulia uwongo *Subhanahu*, Aliye takasika, katika kuhlalisha na kuharimisha, na mengineyo.

34 Na kila umma una ukomo wake maalumu. Na hapana uwezo wowote wa kuupeleka mbele mwisho huo au kuuakhirisha muda wake hata ukiwa mdogo vipi.

35 Enyi wanaadamu! Wakikujieni Mitume kutokana na hiyo jinsi yenu ya kibinaadamu kukufikishieni Ishara zangu zilizo funuliwa nyinyi mnakuwa makundi mawili. Kwa wale wenye kuamini na wakatenda mema kwa usafi wa niya, hapana khofu, wala wao hawatahuzunika katika dunia yao na Akhera yao.

36 Na wale wanao zikanusha hizo Ishara na wakapandwa na kiburi wasizifuata wala wasiongoke kwazo, basi hao ni watu wa Motoni. Humo wataadhibiwa daima milele katika adhabu.

Na watajishuhudia wenyewe kwamba walikuwa makafiri.³⁷

38. Mwenyezi Mungu atasema: Ingieni Motoni pamoja na umma zilizo pita kabla yenu za majini na watu. Kila utakapo ingia umma utawalaani wenzake. Mpaka watakapo kusanyika wote humo, wa mwisho wao watawasema wa mwanzo wao: Mola wetu Mlezi! Hawa ndio walio tupoteza; basi wape adhabu ya Motoni marudufu. Atasema: Itakuwa kwenu nyote marudufu, lakini nyinyi hamjui tu.³⁸

39. Na wa mwanzo wao watawaambia wa mwisho wao: Basi nyinyi pia hamkuwa na ubora kuliko sisi. Basi onjeni adhabu kwa sababu ya mliyo kuwa mkiyachuma.³⁹

40. Hakika wale wanao zikanusha Ishara zetu na wakazifanyia kiburi hawatafunguliwa milango ya mbingu, wala hawataingia Peponi mpaka apite ngamia katika tundu ya sindano. Na hivi ndivyo tunavyo walipa wakosefu.⁴⁰

41. Jahannamu itakuwa kitanda chao na juu yao nguo za moto za kujifunika. Na hivi ndivyo tunavyo walipa madhaalimu.⁴¹

42. Na wale wanao amini na wakatenda mema - hatumkalifishi mtu yoyote ila kwa kiasi cha uwezo wake - hao ndio watu wa Peponi. Wao watadumu humo.⁴²

43. Na tutaondoa chuki vifuani mwao, na mbele yao iwe inapita mito. Na watasema: Alhamdulillah! Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, ambaye aliye tuhidi kufikia haya. Wala hatukuwa wenye kuhidika wenyewe ingeli kuwa Mwenyezi Mungu

37 Hapana wakubwa wa dhulma kuliko hao wanao mzulia Mwenyezi Mungu uwongo, kwa kumnasibisha na mshirika na mwana, na kuzua kuhalalisha na kuharimisha na mengineyo, pasina hoja. Au wanao kanusha Aya, Ishara, za Mwenyezi Mungu zilizo funuliwa katika Vitabu vyake na zinazo onekana katika ulimwengu wake. Hao wanapata hapa duniani sehemu ya aliyo waandikia Mwenyezi Mungu katika riziki, au uhai, au adhabu. Mpaka akiwajia Malaika wa Mauti kuzipokea roho zao, hapo huwaambia kwa kuwasuta: Iko wapi hiyo miungu yenu mliyo kuwa mkiabudu badala ya Mwenyezi Mungu ije kukukingeni na mauti? Nao wajibu: Wametukataa, wametuacha na wametukimbia. Na wajishuhudie wenyewe wakikiri kuwa hakika walikuwa makafiri.

38 Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atawaambia hawa makafiri: Ingieni Motoni pamoja na kaumu nyengine za kikafiri miongoni mwa watu na majini, walio kwisha kutangulieni. Kila umma ukiingia Motoni huwalaani umma mwingine ulio kufuru mfano wao, na ambao waliwafanya ndio wa kuwafuata. Mpaka wakisha ingia kwa kufuatana wote wakakusanyika, wale walio fuata watawashutumu wale walio kuwa waongozi kwa kusema: Ewe Mola wetu Mlezi! Hao walitupoteza tulipo wafuata, kwa kuwa walitutangulia au kwa kuwa walikuwa ndio wakitutawala. Basi wakatugeza kwenye Njia ya Haki tusiifuate. Basi wao wape adhabu mara mbili, wabebe malipo ya uasi wao na uasi wetu! Mwenyezi Mungu atawajibu: Kila mmoja wenu atapata adhabu mara mbili ambayo hapana ataye iepuka katika makundi yenu mawili. Wanao fuata watapata adhabu marudufu kwa ukafiri wao na upotovu wao, na kufuata kwao bila ya kuzingatia na kufikiri. Na wale walio fuatwa watapata adhabu marudufu kwa ukafiri wao na upotovu, na pia kwa kuwakufurisha na kuwapotoa wengineo. Lakini nyinyi hamjui kiasi gani itakuwa adhabu ya kila mmoja wenu.

39 Na hapa tena watasema wale walio fuatwa kuwaambia walio fuata: Kutuiga kwenu sisi katika ukafiri na uasi hakukufanyeni nyinyi muwe bora kuliko sisi hata mstahiki kupunguziwa adhabu! Basi Mwenyezi Mungu atawaambia wote: Onjeni adhabu mlio jiletea wenyewe kwa kuwa mlikuwa mkizua ukafiri na uasi!

40 Hakika wale walio kanusha Ishara zetu zilizo teremshwa katika Vitabu, na ziliopo katika ulimwengu, na wakapanda kiburi kukataa kuhidika kwa Ishara hizo, na wala wasitubu, nawakate tamaa kupokelewa a'mali zao na kupata rehema ya Mwenyezi Mungu, na kuingia Peponi, kama alivyo kata tamaa ngamia kupita katika tundu ya sindano. Na kwa mfano huu ndio tutawaadhibu hao wenye kiburi katika kila umma.

41 Huko katika Jahannamu kitanda chao ni moto, na shuka ya kujifunika ni moto. Na kwa mfano huu tutawaadhibu wanao zidhulumu nafsi zao kwa ukafiri na upotovu.

42 Na wenye kuamini na wakatenda vitendo vyema ambavyo hatumlazimishi ila kwa kiasi anavyo weza mtu, hao ndio watu wa Peponi. Watastarehe humo daima dawamu!

hakutuhidi. Hakika Mitume wa Mola wetu Mlezi walileta Haki. Na watanadiwa kwamba: Hiyo ndiyo Pepo mliyo rithishwa kwa sababu ya mliyo kuwa mkiyafanya.⁴³

44. Na watu wa Peponi watawanadia watu wa Motoni: Sisi tumekuta aliyo tuahidi Mola wetu Mlezi kuwa ni kweli. Je, na nyinyi pia mmekuta aliyo kuahidini Mola wenu Mlezi kuwa ni kweli? Watasema: Ndiyo! Basi mtangazaji atawatangazia: Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate walio dhulumu.⁴⁴

45. Wale ambao walikuwa wakizuilia Njia ya Mwenyezi Mungu, na wakataka kuipotosha, nao wanaikanusha Akhera.⁴⁵

46. Na baina ya makundi mawili hayo patakuwapo pazia. Na juu ya Mnyanyuko patakuwa watu watakao wajua wote kwa alama zao, na wao watawaita watu wa Peponi: Assalamu Alaykum, Amani juu yenu! Wao bado hawajaingia humo, lakini wanatumai.⁴⁶

47. Na yanapo geuzwa macho yao kuelekea watu wa Motoni, watasema: Mola Mlezi wetu! Usitujalie kuwa pamoja na watu walio dhulumu.⁴⁷

48. Na hao watu wa Mnyanyukoni watawaita watu wanao wajua kwa alama zao. Watasema: Kujumuika kwenu hakukufaini kitu, wala hicho mlichu kuwa mnafanyia kiburi.⁴⁸

49. Je, hawa sio wale mlio kuwa mkiwaapia kuwa Mwenyezi Mungu hatawafikishia rehema. Ingieni Peponi, hapana khofu kwenu, wala hamtahuzunika!⁴⁹

43 Na tutazitoa chuki zote ziliomo katika nyoyo zao. Basi watakuwa katika Janna, Pepo, ndugu wenye kupidana, ikipita mito ya maji matamu mbele yao. Watasema kufurahia neema watayo ipata: Alhamdulillah, yaani Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, ambaye aliye tuonyesha Njia ya kufikia neema hizi, na akatuwezesha kuifuata. Na ingeli kuwa hakutuhidi, kutuongoa, Mwenyezi Mungu kwa kutupelekea Mitume na akatupa tawfiq, tusingeweza sisi wenyewe kufikia uwongofu. Hakika Mitume wa Mola wetu Mlezi wametujia na wahyi wa Haki! Hapo tena Mwenyezi Mungu atawaambia: Hakika hii Pepo ni zawadi mmepewa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mmepewa kwa fadhila yangu bila ya kuwa nyinyi kutoa kitu, kama urithi. Na takrima hii mlio pata ni sababu ya vitendo vyenu vyema duniani.

44 Watu wa Peponi watawanadia watu wa Motoni kuwaambia: Sisi tumekwisha ona thwabu alizo tuahidi Mola Mlezi wetu kuwa ni kweli. Je, nyinyi hiyo adhabu aliyo kuahidini Mola Mlezi wenu mmeiona kuwa ni kweli? Nao watajibu: Naam, Ndiyo! Basi mtangazaji atawatangazia watu wa Peponi na watu wa Motoni: Laana, yaani kunyimwa na kufukuzwa kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu, ndio malipo ya wenye kuzidhulumu nafsi zao kwa ukafiri na upotovu.

45 Hawa madhaalimu ndio wanao wazuia watu wasende kwenye Njia ya Mwenyezi Mungu wa Haki, nayo ndiyo Imani na kutenda mema; na wanaweka vikwazo, na shakashaka, ili hiyo Njia yende upogo iwapoteze watu wasiweze kuifuata. Na hao wanaikanusha Akhera hawaiogopi adhabu ya Mwenyezi Mungu.

46 Na baina ya watu wa Peponi na watu wa Motoni patakuwa na pazia kuzuia kufikia kwenye Mnyanyuko - na hapo ni pahala palipo nyanyuka palipo juu. Watu katika bora ya Waumini na watukufu wao, watakuwa wanawaangalia khalaiki wote hao, na wanawajua wema na waovu kwa alama zinazo onyesha ut'iifu wao na uasi wao. Wataitwa watu wema kabla ya kuingia Peponi, na hali wao wanataraji kuingia humo, watawabashiria kwa Imani na utulivu na kuingia Peponi.

47 Macho ya hao Waumini yakigeukia upande wa watu wa Motoni baada ya wito huo, watasema kwa kitisho watacho kiona cha Moto: Ewe Mola wetu Mlezi! Usitutie pamoja na hawa madhaalimu walio dhulumu nafsi zao, wakadhulumu Haki, na wakawadhulumu watu!

48 Na wale watu wa daraja za juu katika Pepo, nao ni Manabii, na *Mas'iddiqina*, watawaita walio kuwa wakiwajua kwa sifa zao katika watu wa Motoni, wakisema kwa kuwalaumu: Huko kujumuika kwenu kwa wingi, hakukufaini chochote, wala huko kupanda kiburi kuikataa Haki kwa kutegemea ujamaa wenu na utajiri wenu. Na hivi sasa mnawaona hawa, nini hali yao na nini hali yenu.

49 Hao wanyonge mlio kuwa mkiwadharau, na mkaapa kuwa hayumkini Mwenyezi Mungu awateremshie

50. Na watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi: Tumimieni maji, au chochote alichokuruzukuni Mwenyezi Mungu. Nao watasema: Hakika Mwenyezi Mungu ameviharimisha hivyo kwa makafiri,⁵⁰

51. Ambao waliifanya dini yao kuwa ni pumbao na mchezo, na maisha ya dunia yakawadanganya. Basi leo Sisi tunawasahau kama walivyo usahau mkutano wa Siku yao hii, na kwa sababu ya kule kuzikataa Ishara zetu.⁵¹

52. Na hakika tumewaletea Kitabu tulicho kipambanua kwa ilimu, uwongofu na rehema kwa watu wenye kuamini.⁵²

53. Je, lipo wanalo lingojea isipo kuwa matokeo yake? Siku yatapo fika matokeo yake watasema wale walio kisahau: Kweli Mitume wa Mola Mlezi wetu walileta Haki! Je, tunao waombezi ili watuombe? Au turudishwe ili tufanye yasiyo kuwa yale tuliyo kuwa tukiyafanya? Bila ya shaka wamejikhasiri nafsi zao, na yamewapotea waliyo kuwa wakiyazua.⁵³

54. Hakika Mola Mlezi wenu ni Mwenyezi Mungu aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha akatawala juu ya Kiti cha Enzi. Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua, na mwezi, na nyota zinazo tumika kwa amri yake. Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.⁵⁴

rehema, kama kwamba nyinyi ndio mnao ishika rehema yake, wao wamekwisha ingia Peponi! Na Mola wao Mlezi atawaambia: Ingieni humo kwa amani. Hapana khofu juu yenu kwa jambo lolote litalo kupatieni, wala hamtahuzunika kwa jambo mlilo likosa.

50 Na watu wa Motoni watawanadia watu wa Peponi kwa kuwaambia: Hebu twachilieni maji kidogo yatumimini sisi, au tugaieni kitu katika vyakula na mavazi na starehe nyengine alizo kupeni Mwenyezi Mungu Mtukufu! Nao watu wa Peponi watawajibu: Sisi hatuwezi kufanya hayo, kwa sababu Mwenyezi Mungu amezuia vyote hivyo wasipate watu wapinzani, walio mkanusha Yeye na neema zake katika dunia.

51 Hawa makafiri ndio ambao hawakufanya juhudi kutafuta Dini ya Haki, lakini ikawa dini yao ni kufuata pumbao na matamano, ndio pumbao la kujipumbazia na upuuzi wa kuchezea, na maisha ya dunia na anasa zake zikawakhadada, wakadhania hayo tu ndiyo maisha, na wakasahau kukutana nasi! Basi Siku ya Kiyama Sisi tutawasahau. Na wao hawato istarehea Pepo, na watauonja Moto, kwa sababu ya sahadu yao kuisahau Siku ya Kiyama, na kuzikanusha Ishara zenye kubainika wazi, zinazo thibitisha Haki.

52 Na hakika kwa ajili ya kubainisha Haki tuliwapa Kitabu, na tukakipambanua. Kitabu hicho kimekusanya ilimu nyingi, na ndani yake zimo hoja za Tawhid, Upweke wa Mwenyezi Mungu, na Ishara za Mwenyezi Mungu katika ulimwengu; na pia zimo sharia zake, maelezo ya Njia Iliyo Nyooka, na uwongofu wa kuifikilia. Na pia yamo ndani ya Kitabu hichi mambo ambayo, lau watu wakiyafuata watapata rehema. Na wala hawanufaiki kwacho ila wale ambao ni shani yao kuinyenyekea Haki na kuamini.

53 Hakika wao hawaiamini hii Qur'ani, na wala hawangojei ila matokeo ambayo Mwenyezi Mungu ameyabainisha kuwa yatawapata wanayo ikataa! Na Siku yatapofika hayo matokeo, nayo ni Siku ya Kiyama, walio ziacha amri zake na maelezo yake, na wakaghafilika kuwa ni waajibu kuamini, na hali wakiungama madhambi yao, watasema: Hakika walikuja Mitume kutoka kwa Muumba wetu na Mlezi wetu, wakituitia Haki waliyo tumwa kuileta, nasi tukaikataa! Nao wataulizwa: Je, mnao waombezi wakakuombeeni? Nao hawatowapata! Au, je, watarudishwa tena duniani watende mema? Hawatajibiwa! Wamepoteza vitendo vyao kwa kukhadaika na dunia, na memewapotea ule uzushi wa uwongo wa kudai kuna mungu asiye kuwa Allah, Mwenyezi Mungu.

54 Hakika Mola Mlezi wenu ambaye Mitume wake wanakuiteni mwende kwenye Haki, na kuamini Siku ya Mwisho na Malipo, ndiye Muumba ulimwengu, naye ndiye aliye uanza. Kaumba mbingu na ardhi kwa viwango sita, vinavyo shabihiana na siku sita, katika siku za dunia. Kisha akatawala juu ya Ufalme ulio kamilika. Naye ndiye anaye ufanya usiku uufunike mchana kwa kiza chake, na usiku unafuatia mchana kwa upesi na mpango na kufuatana kusikosita, kama anavyo taka Yeye. Naye Mwenyezi Mungu Subhana ameliumba jua, na mwezi, na nyota. Na vyote hivyo vinamnyenyekea Mwenyezi Mungu Mtukufu, vinakwenda kwa amri yake. Na Yeye peke yake ndiye Mwenye kuumba na Mwenye amri ya kuitikiwa.

- 55.** Muombeni Mola wenu Mlezi kwa unyenyekevu na kwa siri. Hakika Yeye hawapendi warukao mipaka.⁵⁵
- 56.** Wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwisha tengenezwa. Na muombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanao fanya mema.⁵⁶
- 57.** Na Yeye ndiye anaye peleka pepo (za kuvuma) kuwa ni bishara kabla ya kufika rehema yake. Hata hizo pepo zinapo beba mawingu mazito tunayachunga mpaka kwenye nchi iliyo kufa. Kisha tunateremsha kwayo maji, ndio kama hivyo tukatolesha kila aina ya matunda. Basi hali kadhaalika tunavyo wafufua wafu, ili mpate kukumbuka.⁵⁷
- 58.** Na ardhi njema, yenye udongo wa rutba, hutoa mimea yenye kukua vizuri yenye uhai, kwa idhini ya Mola Mlezi wake. Na ardhi mbaya haitoi ila mimea michache, isiyo na faida, tena kwa shida. Na hivyo ndivyo tunavyo zipambanua Ishara (Aya) kwa watu wanao shukuru.⁵⁸
- 59.** Tulimpeleka Nuhu kwa kaumu yake, naye akasema: Enyi kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyo kuu.⁵⁹
- 60.** Wale watukufu katika kaumu yake wakasema: Hakika sisi tunakuona wewe umo katika upotofu ulio dhaahiri.⁶⁰
- 61.** Akasema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika upotofu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.⁶¹

Baraka za Mwenye kuanzisha ulimwengu na viliomo ndani yake zimetukuka. (*Tazama Maelezo 7:54*)
55 Iliyokuwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu, ndiye aliye umbra kila kitu peke yake, basi muombeni Yeye tu kwa kumuabudu na kwa mengineyo, mkimtangazia hayo maombi, kwa udhalilifu na kunyenyekeka, kwa dhaahiri au bila ya kudhihirisha. Wala msipite mipaka kwa kumshirikisha na wengine, au kwa kumdhulumu yeyote. Kwani hakika Mwenyezi Mungu, hawapendi wanao ruka mipaka, na wafanyao uadui.

56 Wala msifanye fisadi katika nchi njema kwa kueneza maasi na dhulma na uvamizi. Na muombeni Yeye *Subhanahu*, Aliye takasika, kwa kuiogopa adhabu yake, na kwa kutumai thawabu zake. Na hakika rehema yake ipo karibu kwa kila mwenye kufanya mema. Na hayo ni hakika.

57 Na Mwenyezi Mungu, Aliye takasika, Aliye tukuka, peke yake, ndiye anaye zipeleka pepo kubashiria rehema yake, kwa mvua ambazo kwa sababu yake ndio makulima humea, na konde humwagiwa maji. Hizo pepo hubeba mawingu ambayo nayo yamebeba maji. Tunayachunga mpaka yafike kwenye nchi isiyo kuwa na mimea, ambayo ni kama maiti asiye na uhai, yakamiminika maji, na tena Mwenyezi Mungu husababisha kumea namna kwa namna ya mazao na matunda. Na mfano kama huu wa kuihuisha ardhi kwa mimea, ndivyo tunawafanya maiti wakawa wahai. Haya ni kwa ajili mpate kuikumbuka kudra ya Mwenyezi Mungu, na mpate kuamini kuwa kupo kufufuliwa.

58 Na ardhi njema yenye rutba nzuri huzalisha mimea inayo kua kwa nguvu, kwa idhini ya Mola Mlezi. Na ardhi mbaya haitoi ila mimea michache, isiyo na faida, ambayo huwa ndio sababu ya dhiki ya huyo mkulima.

59 Washirikina wakafanya inda, na wakaikanusha Haki ilipo wajia kwa hoja za kukata zisio pingika. Lakini huo ndio mtindo wa makafiri kwa Manabii wao tangu zamani. Sisi tulimtuma Nuhu kwa watu wake alio tokana nao. Naye akawakumbusha kuwa yeye ni mmoja wao: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake. Kwani nyinyi hamna Mungu asiye kuwa huyu. Na mjue kuwa kutakuwapo kufufuliwa na kuhisabiwa Siku ya Kiyama. Na hiyo ni Siku adhimu. Mimi nakukhofieni Siku hiyo msije mkapata adhabu kali kweli.

60 Wakasema wale wahishimiwa wao, watu wa mbele mbele na uwongozi katika wao, wakiujibu ule wito wake wa Tawhidi na Siku ya Akhera: Hakika sisi tunakuona wewe uko mbali kabisa na hiyo haki.

61 Nuhu akawaambia kukataa yale waliyo msingizia: Mimi sina upotofu kama mnavyo dai. Lakini mimi

62. Nakufikishieni Ujumbe wa Mola Mlezi wangu, na ninakunasihini; na ninayajua kwa Mwenyezi Mungu msiyo yajua nyinyi.⁶²

63. Je, mnastaajabu kukujieni mawaidha yanayotoka kwa Mola Mlezi wenu kwa njia ya mtu aliye ni mmoja katika nyinyi, ili akuonyeni na ili mumchemngu, na ili mpate kurehemewa?⁶³

64. Basi walimkanusha. Nasi tukamwoko ya yeye na walio kuwa pamoja naye katika jahazi. Na tukawazamisha wale walio kanusha Ishara zetu. Hakika hao walikuwa watu vipofu.⁶⁴

65. Na kwa A'adi tulimpeleka ndugu yao, Hud. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mungu ila Yeye. Basi je, hamumchi?⁶⁵

66. Wakasema watukufu wa wale walio kufuru katika kaumu yake: Sisi tunakuona umo katika upumbavu, na hakika sisi tunakufikiria kuwa wewe ni katika waongo.⁶⁶

67. Akasema: Enyi watu wangu! Mimi sina upumbavu. Lakini mimi ni Mtume niliye toka kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.⁶⁷

68. Nakufikishieni ujumbe wa Mola wangu Mlezi. Na mimi kwenu ni mwenye kukunasihini, muaminifu.⁶⁸

69. Mnaona ajabu kukufikieni mawaidha yanayo toka kwa Mola wenu Mlezi kwa mtu aliye mmoja wenu nyinyi ili akuonyeni? Na kumbukeni alivyo kufanyeni mshike pahala pa kaumu ya Nuhu, na akakuzidisheni katika umbo. Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.⁶⁹

ni Mtume niliye toka kwa Muumba wa viumbe vyote, basi hayumkini awe mbali na haki.

62 Na mimi katika huu wito wa Haki mshike Tawhidi na kuamini Siku ya Mwisho, nafikisha Ujumbe aliyo nituma Mwenyezi Mungu, nao mfuata hukumu za Mwenyezi Mungu ambazo ndizo zinazo msilili mwanaadamu. Na mimi nakupeni nasaha ya kweli itokayo kwenye moyo wangu ulio safi. Na Mwenyezi Mungu amenifunza mambo ambayo nyinyi hamyajui.

63 Mnanizulia kuwa nimepotea na kuwa nipo mbali na Haki? Na mnastaajabu kukujieni kumbusho kutokana na Mwenyezi Mungu aliye kuumbeni kwa ulimi wa mtu aliye kuja kwenu kukuonyeni adhabu pindi mkikanusha, na akakuiteni mwende kuufuata uwongofu, na kutengeza nyoyo, na kujiepusha na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutaraji muwe katika rehema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu duniani na Akhera? Haifai kuwa mnastaajabu na mnakanusha juu ya kuwepo hoja zenye kuthibitisha Utume huu.

64 Lakini wao juu ya hoja hizo zilizo wazi wengi wao hawakuamini, bali walimkanusha. Kwa hivyo tukawateremshia adhabu ya kuwazamisha katika maji, na tukawaokoa wale walio amini katika jahazi alilo liunda kwa kuongozwa nasi. Na wakazama wale walio kanusha juu ya kuwapo hoja zilizo wazi, nao wakafanya inda wakawa hawaioni Haki kwa kuwa walipofuka wasiione.

65 Kama tulivyo mtuma Nuhu kwa kaumu yake kuwalingania Tawhidi, kadhaalika tuliwatumia kina 'Aad Nabii Hud, naye ni mmoja wao, makhusiano yake nao ni kama ndugu kwa ndugu. Akawaambia: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu peke yake, nanyi hamna Mungu asiye kuwa Yeye. Na hii ndiyo njia ya kujikinga na shari na adhabu. Nayoy ndiyo Njia Iliyo Nyooka. Basi je, mtaifuata njia mjikinga na shari na upotovu? (*Tazama Maelezo 7:65*)

66 Wakasema wenye uwongozi na umbele mbele katika kaumu yake: Sisi tunakuona umepungukiwa na akili, kwa kutuitia wito huu; na tunaitakidi kuwa wewe ni mwongo.

67 Akasema: Enyi watu wangu! Katika wito huu sina upungufu wa akili hata chembe, wala mimi si mwongo. Lakini mimi nimekuja na uwongofu, na mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, naye Yeye ndiye Mola Mlezi wa viumbe vyote.

68 Katika haya ninayo kwambieni mimi nafikisha amri na makatazo ya Mola Mlezi wangu, na hayo ndio Ujumbe wake kwenu. Na mimi nakupeni nasaha ya dhati, kwa niya safi kabisa. Na mimi ni muaminifu katika ninayo kwambieni, wala mimi si miongoni ya watu waongo.

69 Tena Hud akawaambia: Hivyo mmestaajabu mno, na mkaona mageni kukujieni ukumbusho wa Haki

70. Wakasema: Je! Umetujia ili tumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake, na tuyaache waliyo kuwa wakiyaabudu baba zetu? Basi tulettee hayo unayo tuahidi, ukiwa miongoni mwa wasemao kweli.⁷⁰

71. Akasema: Bila ya shaka adhabu na ghadhabu zimekwisha kukuangukieni kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Mnabishana nami kwa ajili ya majina tu mliyo yaita nyinyi na baba zenu ambayo kwayo Mwenyezi Mungu hakuteremsha uthibitisho? Basi ngojeni, mimi pia ni pamoja nanyi katika wanao ngoja.⁷¹

72. Basi tukamwokoia yeye na walio kuwa pamoja naye kwa rehema zetu, na tukakata mizizi ya wale walio zikanusha Ishara zetu, na hawakuwa wenye kuamini.⁷²

73. Na kwa Thamud tulimpeleka ndugu yao, Saleh. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Hakika imekwisha kukufikieni Ishara iliyo wazi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Huyu ni ngamia jike wa Mwenyezi Mungu aliye ni Ishara kwenu. Basi mwachieni ale kwenye ardhi ya Mwenyezi Mungu, wala msimdhuru, isije kukushukieni adhabu chungu.⁷³

74. Na kumbukeni alivyo kufanyeni wa kushika pahala pa A'adi na akakuwekeni vizuri katika nchi, mnajenga majumba ya fakhari katika nyanda zake, na mnachonga majumba katika milima. Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu wala msitende uovu katika nchi kwa ufasidi.⁷⁴

kwa ulimi wa mtu aliye mmoja wenu, kukuonyeni? Mkiendelea na haya mliyo nayo matokeo yake yatakuwa ni mabaya mno. Na hakika jambo hilo si la kustaajabiwa. Kisha Hud akawatajia yaliyo wasibu walio kanusha katika watu walio watangulia, na akawakumbusha neema za Mwenyezi Mungu juu yao. Akasema: Kumbukeni Mwenyezi Mungu alivyo kufanyeni ndio warithi wa nchi baada ya kaumu ya Nuhu alio waangamiza kwa kumkadhibisha Nuhu, na Mwenyezi Mungu akakuzidishieni nyinyi nguvu za mwili na nguvu za utawala. Na neema hizo zinatajikana zilete Imani. Basi zikumbukeni neema zake ili mpate kufuzu.

70 Lakini wao juu ya wito mzuri huu walisema kwa kuona mageni: Hivyo wewe umetujia kututaka tumuabudu Mwenyezi Mungu mmoja peke yake, na tuache masanamu waliyo kuwa wakiyaabudu baba zetu? Na hapana shaka sisi hatutofanya hayo, nawe tulettee hiyo adhabu unayo tutishia, kama wewe kweli ni katika wasema kweli.

71 Hakika kwa hii inadi yenu mmestahiki adhabu ya Mwenyezi Mungu ikuteremkieni, na ghadhabu yake ikufikieni! Nyinyi mnabisha kwa ajili ya masanamu ambayo mliyo yaita kuwa ni miungu nyinyi na baba zenu, na wala si chochote ila ni majina tu walio pewa, na wala Mwenyezi Mungu hakuleta hoja ya kuonyesha ungu wao. Hayo hayana nguvu za muumbaji inayo kuruhusuni kuyaabudu! Na ikiwa mtashikilia ukaidi huu basi ingojeeni adhabu ya Mwenyezi Mungu, nami pamoja nanyi, sote tungoje nini kitakushukieni.

72 Basi Sisi tukamwokoia A'ad na walio amini pamoja naye kwa rehema yetu, na tukawateremshia makafiri cha kuwateketeza, na hapana chao kilicho bakia wala hapana athari yao, na wala hawakuingia katika kundi la Waumini.

73 Na tuliwapelekea kina Thamud ndugu yao Saleh, ambaye ni mwenzi wao kwa nasaba na uwananchi. Na wito wake ulikuwa kama wito wa Mitume walio kuwa kabla yake na baada yake. Akawaambia: Msafishieni ibada Mwenyezi Mungu peke yake, na wala hapana Mungu isipo kuwa Yeye. Na hoja ya Utume wangu imekwisha kukujilieni kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Nayo ni huyo ngamia mwenye sifa za pekee. Katika huyo ngamia pana hoja. Yeye ni ngamia wa Mwenyezi Mungu, muacheni ale atakapo katika ardhi ya Mwenyezi Mungu, wala msimdhuru isije kukupateni adhabu chungu. (Tazama Maelezo 7:73)

74 Na kumbukeni kuwa Mwenyezi Mungu amekujaalieni ndio wa kurithi nchi ya A'ad, na akakupeni katika hiyo nchi makaazi mema, mkijenga majumba ya fakhari katika nyanda zake. Na mkichonga milima mkifanya majumba. Basi kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu, alivyo kuwekeni kwa makini katika nchi, wala msifanye maovu katika nchi, mkawa wenye kufisidi na kuharibu baada ya kukaa kwa makini kama huku.

75. Waheshimiwa wa kaumu yake wanao jivuna waliwaambia wanao onewa wenye kuamini miongoni mwao: Je, mnaitakidi ya kwamba Saleh ametumwa na Mola Mlezi wake? Wakasema: Hakika sisi tunayaamini yale aliyo tumwa.⁷⁵

76. Wakasema wale wanao jivuna: Sisi tunayakataa hayo mnayo yaamini.⁷⁶

77. Na wakamuwa yule ngamia, na wakaasi amri ya Mola Mlezi wao, na wakasema: Ewe Saleh! Tuletee unayo tuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa Mitume.⁷⁷

78. Basi tetemeko la ardhi likawanyakua, na kulipo kucha wakawa majumbani mwao kifudifudi wamekwisha kufa.⁷⁸

79. Basi Saleh akwaacha na akasema: Enyi watu wangu! Nilikufikishieni Ujumbe wa Mola wangu Mlezi, na nikakunasihini, lakini nyinyi hamwapendi wenye nasaha.⁷⁹

80. Na tulimtuma Lut', alipo waambia watu wake: Je, mnafanya uchafu ambao hajakutangulieni yeyote kwa uchafu huo katika viumbe vyote!⁸⁰

81. Hivyo nyinyi mnawaingilia wanaume kwa matamanio mkwawacha wanawake? Kumbe nyinyi ni watu wafujaji!⁸¹

82. Na haikuwa jawabu ya kaumu yake isipo kuwa kuambizana: Wafukuzeni katika mji wenu, maana hao ni watu wanao jitakasa.⁸²

83. Basi tukamwoko ya yeye na watu wake, isipo kuwa mkewe, alikuwa miongoni mwa walio bakia nyuma.⁸³

84. Na tukawamiminia mvua. Basi tazama jinsi ulivyo kuwa mwisho wa wakosefu.⁸⁴

75 Wale wenye kiburi katika watu wa mbele-mbele na uwongozi waliwasemeza wanyonge kwa kuwalaumu na kuwadhalilisha: Hivyo nyinyi mnaitakidi kuwa kweli Saleh ametumwa na Mola Mlezi wake? Watu wa Haki wakawajibu: Sisi tunaitakidi na tunakubali aliyo tumwa kwetu.

76 Wakasema wenye kiburi: Sisi tunapinga na tunayakataa hayo mnayo yaamini nyinyi, na hayo anayo itia Saleh ya kuwa Mungu ni mmoja.

77 Inda ya wenye kiburi ikakakamia, na wakampinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakamchinja Ngamia. Walivuka mpaka katika kiburi chao, wakaitupilia mbali amri ya Mola wao Mlezi, na wakasema kwa upinzani: Ewe Saleh! Tuletee hiyo adhabu uliyo tuahidi ikiwa kweli wewe ni miongoni ya alio watuma Mwenyezi Mungu.

78 Tetemeko la nguvu lilikuja kuwanyakua, na kulipo pambazuka wakawa wote wamekwisha jifa majumbani mwao wamejifudikiza kifudifudi.

79 Na kabla ya kuwateremkia adhabu hiyo ndugu yao Saleh aliwaachilia mbali (kwa kukata tamaa nao), akawaambia: Enyi watu wangu! Mimi nimekufikishieni amri na makatazo ya Mola Mlezi wangu. Na nimekusafeni nasaha yangu, lakini nyinyi kwa ushindani wenu na ushupavu wenu, mmekuwa hamupendi anaye kunasihini!

80 Na hakika tulimtuma Nabii wa Mwenyezi Mungu, Lut', kwa kaumu yake; awaite wafuate Tawhidi, yaani ibada ya Mwenyezi Mungu mmoja. Na awazindue juu ya waajibu wa kuachana na makosa maovu kabisa waliyo kuwa wakiyafanya. Aliwaambia: Nyinyi mnakwenda kufanya jambo lilio pita mpaka kwa ubaya wake, kinyume na maumbile? Mmezua uchafu huo ambao unapingana na khulka, na ambao hapana watu walio kutangulieni walio fanya hayo.

81 Na jambo hilo ni kuwa mnawaendea wanaume kwa kuwatamani, na mnawawacha wanawake! Nyinyi kwa jambo hili inakuwa mnafanya fujo, na mmetoka nje ya maumbile, na mmefanya kitendo asicho fanya hata mnyama.

82 Na haikuwa jawabu ya watu wake kwa kukatazwa hichi kitendo kiovu kisicho kuwa na mfano, ila ni kusema: Watoeni Lut' na jamaa zake na wafuasi wake katika mji wenu! Nayo ni kwa kuwa wao wanajitahirisha na wanajitenga na hichi kitendo ambacho akili na maumbile yanakiona ni kibaya, na wao hao watu wanakioni kizuri!

83 Amri ya kuadhibiwa ilikwisha thibiti. Basi Sisi tukamwoko Lut' na watu wake, isipo kuwa mkewe, kwani yeye alikuwa katika hao walio potea.

84 Basi tuliwateremshia mvua ya mawe ya kuteketeza, na ardhi ikatandazwa kwa mitetemeko ya chini yao! Basi ewe Nabii! Angalia vipi ulikuwa mwisho wa wakosefu.

85. Na kwa watu wa Madyana tulimtuma ndugu yao Shua'ib. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Hamna mungu mwengine isipo kuwa Yeye. Imekwisha kufikieni hoja wazi kutoka kwa Mola Mlezi wenu. Basi timizeni sawasawa vipimo na mizani, wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye uharibifu katika nchi, baada ya kuwa imekwisha tengenea. Hivi ndivyo bora kwenu ikiwa nyinyi ni Waumini.⁸⁵

86. Wala msikae katika kila njia mkitisha watu, na kuwazuilia na Njia ya Mwenyezi Mungu wale wenye kumuamini, na mkataka njia ipotoke. Na kumbukeni mlipo kuwa wachache, naye akakufanyeni kuwa wengi. Na tazameni jinsi ulivyo kuwa mwisho wa mafisadi.⁸⁶

87. Na kama liko kundi miongoni mwenu lililo amini haya niliyo tumwa, na kundi jengine halikuamini, basi subirini mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu baina yetu. Naye ndiye Mbora wa wenye kuhukumu.⁸⁷

88. WAHESHIMIWA WALIO TAKABARI katika kaumu yake wakasema: Ewe Shua'ib! Tutakutoa wewe pamoja na wale walio kuamini katika mji wetu, au mrejee katika mila yetu. Akasema: Je, ingawa tunaichukia?⁸⁸

89. Bila ya shaka itakuwa tumemzulia uwongo Mwenyezi Mungu tukirudi katika mila yenu baada ya kwisha tuokoa nayo Mwenyezi Mungu. Wala haiwi kwetu sisi kuirejea mila hiyo, ila akitaka Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wetu. Ujuzi wa Mola Mlezi wetu umeenea katika kila kitu. Kwa Mwenyezi Mungu tunategemea. Ewe Mola Mlezi wetu! Tuhukumie baina yetu na kaumu yetu kwa haki, nawe ndiye mbora wa wanao hukumu.⁸⁹

85 Na kwa watu wa Madyana tulimtuma ndugu yao, Shua'ib. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu peke yake. Kwani nyinyi hamna mungu isipo kuwa Yeye. Hoja zilizo wazi za kuthibitisha Haki inayo toka kwa Mola Mlezi wenu juu ya Utume wangu kwenu zimekwisha kujieni. Na umekujieni Ujumbe wa Mola wenu Mlezi kwamba mtengeneze kwa uadilifu maingiliano yenu nyinyi kwa nyinyi. Basi timizeni vipimo na mizani mnapo uziana, wala msipunguze haki za watu, wala msiharibu nchi nzuri, kwa kufisidi mapando na kadhaalika, na kuwatenga jamaa na kuondoa mapenzi. Kwani hayo ni bora kwenu mkiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, na mnaamini Haki iliyo wazi.

86 Wala msikae katika kupinga kila njia za Haki na uwongofu na a'mali njema, mkiwatishia wapitao, na kwa hivyo mkawazulia watafutao kheri wasiifikie. Nao hao ndio watu wa Imani wanao muamini Mwenyezi Mungu, nanyi mnaitaka njia iliyo potoka! Na kumbukeni mlivyo kuwa ni watu wachache, Mwenyezi Mungu akakufanyeni mkawa wengi kwa kwenda sawa kutaka uzazi na mali. Na zingatieni nini ulikuwa mwisho wa uharibifu walio kuwa kabla yenu.

87 Ikiwa kipo kikundi kati yenu kilicho amini Haki niliyo kuja nayo, na kikundi kingine hakikuamini, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete hukumu yake baina ya pande mbili hizo. Naye ndiye Mbora wa mahakimu.

88 Hii ni khabari ya Shua'ib katika wito wake kuwalingania kaumu yake. Ama hao kaumu yake walikuwa wamemili juu ya upotovu. Na wale wakubwa wao walio takabari waliukataa wito, na wakaona ni uvunjifu kuifuata Haki. Wakamkabili Shua'ib kumwambia dhamiri yao kwa kusema: Hakika hapana vingine ila tukutoe wewe na hao walio amini pamoja nawe katika mji wetu. Na tutakufukuzeni, wala hamtasalimika na adhabu hii ila mkirejea katika hii dini yetu mliyo iacha. Shua'ib a.s. akawajibu kwa kusema: Turejee katika mila yenu na hali sisi tunaichukia kwa uharibifu wake? Hayawi hayo abadan!

89 Akaendelea zaidi kuwavunja tamaa yao ya kuwarejeza kwenye mila yao kama walivyo taka. Akasema: Tutakuwa tunamzulia uwongo Mwenyezi Mungu tukiwa katika mila yenu baada ya Mwenyezi Mungu kesho tuhidi kwenye Njia Iliyo Nyooka. Na haifai sisi kuwa katika mila yenu kwa khiari yetu na kutaka kwetu, ila akipenda Mwenyezi Mungu turejee katika mila yenu. Na hayo hayawi! Kwa sababu Mola Mlezi wetu anatumia vyema, na Yeye hataki turejee kwenye upotovu wenu. Yeye aliye tukuka shani yake amekienea kila kitu kwa ujuzi wake. Anatuongoa kwa upole wake na hikima yake kwenye jambo litalo

90. Na waheshimiwa walio kufuru katika kaumu yake wakasema: Mkimfuata Shua'ib, basi hakika hapo nyinyi mtakuwa mlio khasiri.⁹⁰

91. Basi tetemeko la ardhi likawanyakua, na wakaamkia majumbani mwao wamejifudikiza, wamekwisha kufa.⁹¹

92. Wale walio mkanusha Shua'ib wakawa kama kwamba hawakuwako. Walio mkanusha Shua'ib ndio walio kuwa wenye kukhasiri.⁹²

93. Basi akawaachilia mbali na akasema: Enyi kaumu yangu! Nimekufikishieni Ujumbe wa Mola Mlezi wangu, na nimekunasihini; basi vipi niwahuzunikie watu makafiri?⁹³

94. Na hatukumtuma Nabii yeyote katika mji ila tuliwapatiliza wakaazi wake kwa taabu na mashaka ili wapate kunyenyekea.⁹⁴

95. Kisha Sisi hubadilisha mahala pa ubaya kwa wema, hata wakazidi, na wakasema: Taabu na raha ziliwafikia baba zetu. Basi kwa ghafla tukawashika, hali ya kuwa hawajatambua.⁹⁵

tuhifadhia Imani yetu. Kwa Yeye peke yake ndio tumesalimisha mambo yetu, na huku tunashikilia yale aliyo tuwajibisha tuyashike. Ewe Mola Mlezi wetu! Tutenge sisi na hao kaumu yetu kwa Haki, kama ilivyo kuwa mwendo wako unavyo amua baina ya wenye kufuata Haki na wakatenda mema, na wale wapotovu waharibifu. Na Wewe kwa kuwa ujuzi wako na uwezo ulivyo enea ndiye Muadilifu na Muweza kuliko mahakimu wote.

90 Hapo basi wale watu walikata tamaa ya kuwafanya Shua'ib na walio kuwa naye wawafuate wao. Na wakajua kuwa hakika hao walikuwa wamethibiti katika Dini yao. Kadhaalika waliogopa wasizidi kuwa wengi wale walio hidika pamoja na Shua'ib kwa kudhihiri nguvu zake na kuthibiti kwake juu ya wito wake. Kwa hivyo wale waheshimiwa wa kikafiri wakawaelekea wafwasi wao wakiwatisha kwa kusema: Wallahi! Mkimfuata Shua'ib mkakubali wito wake, basi hapana shaka nyinyi utakutokeni utukufu wenu na utajiri wenu kwa kufuata dini potovu wasio kuwa wakiifuata wazee wenu.

91 Basi hapo kauli ya kuteremka adhabu ikawa imethibiti. Wakasibiwa kwa tetemeko lilio tikisa nyoyo zao, wakawa katika majumba yao wamesinukia kifudifudi hawana tena uhai.

92 Hii ndio shani ya Mwenyezi Mungu na hao walio mkanusha Shua'ib, na wakamtishia, na wakamwonya kuwa watamfukuza katika mji wao, na wakafanya kila kitu kuupinga wito wake. Wamehiliki wao na ukahiliki mji wao, ikawa kama kwamba humo hawakuwahi kuishi wale walio mkadhibisha Shua'ib na wakadai kuwa ati atakaye mfuata atakuwa amekhasiri, na wakatilia nguvu madai hayo. Na lililo kuwa ni kuwa wao ndio walio poteza neema yao ya dunia na Akhera.

93 Shua'ib alipo ona hilaki ya kuvuruga iliyo wateremkia wale watu, basi aliwaachilia mbali, na akasema kujivua nafsi yake asiwe mkosa pamoja nao: Mimi nimekufikishieni ujumbe wa Mola wenu Mlezi unao pelekea mpate wema nyinyi, lau kuwa mngeli ufuata. Na mimi nimefanya ukomo wa uwezo wangu katika kukunasihini, na kukuwaidhini kwa mambo ya kukuokoeni na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Basi vipi tena niwasikitikie mno watu makafiri? Hayawi hayo baada ya kuwa mimi nimekwisha jiidhuru kwao, na nikatumia juhudi yangu kwa ajili ya kutaka kuwahidi na kuwaokoa, na wao wakakhiari kufuata yale yale ya kuwahiliki.

94 Na Sisi hatukumpeleka Nabii yeyote kwenye mji akawalingania watu wake wafuate Dini ya Mwenyezi Mungu iliyo sawa, na wao wakakataa kuukubali huo wito, ila tuliwapatiliza kwa ufakiri na maradhi, ili wapate kuwa wanyonge na wamwombe Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu, na kumsafia niya wapate kuondokewa na balaa na wamuitikie Mtume wake.

95 Basi tena ilivyo kuwa hawakufanya hayo, bali wakaendelea na ukafiri wao na inadi yao, tukawapa mtihani wa kuwapa neema badala ya dhiki ili kuwapururia tu. Tukawapa kutoonoka, na nafasi nzuri, na siha na afya, mpaka wakawa wengi, na mali yao yakazidi, wakasema kwa ujinga wao: Hayo yaliyo wapata baba zetu ya mahna, na balaa, na starehe na neema - hayo yote ndio shani ya ulimwengu. Shida na neema huwajia watu kwa zamu. Hawakuzindukana wakajua kuwa haya ni malipo ya kufuru zao wakajizua! Na kwa hivyo wakawa hawajui mwendo wa Mwenyezi Mungu, iliyo tukuka shani yake, katika sababu za matengenezo na uharibifu wa binaadamu, na nini linalo leta neema na nini linalo leta dhiki! Matokeo ya hayo ni kuwa Mwenyezi Mungu aliwapatiliza kwa kuwaletea adhabu ya kuteketeza kwa ghafla, na wao bila ya kujua nini litawafika.

96. Na lau kuwa watu wa miji wangueli amini na wakamchamngu, kwa yakini tungeli wafungulia baraka kutoka mbinguni na katika ardhi. Lakini walikanusha basi tukawapatiliza kwa sababu ya yale waliyo kuwa wakiyachuma.⁹⁶

97. Je, watu wa mijini wameaminisha ya kuwa adhabu yetu haitawafika usiku, nao wamelala?⁹⁷

98. Au watu wa mijini wameaminisha ya kuwa adhabu yetu haitawafika mchana, nao wanacheza?⁹⁸

99. Je, wamejiaminisha na mipango ya Mwenyezi Mungu? Kwani hawajiaminishi na mipango ya Mwenyezi Mungu ila watu wenye kukhasiri.⁹⁹

100. Je, hawahidiki hawa wanao rithi ardhi baada ya wale wenyewe kwamba tukitaka tutawapatiliza kwa madhambi yao, na tutapiga muhuri juu ya nyoyo zao, na kwa hivyo hawatasikia?¹⁰⁰

101. Miji hiyo, tunakusimulia baadhi ya khabari zake. Na hapana shaka Mitume wao waliwafikia kwa hoja zilizo waziwazi. Lakini hawakuwa wenye kuamini waliyo yakanusha zamani. Namna hivi Mwenyezi Mungu anazipiga muhuri nyoyo za makafiri.¹⁰¹

102. Wala hatukuwaona wengi wao kuwa wanatimiza ahadi; bali kwa hakika tuliwakuta wengi wao ni wapotofu.¹⁰²

103. Kisha baada yao tukamtuma Musa na Ishara zetu kwa Firauni na waheshimiwa

96 Na lau kuwa watu wa hiyo miji wangueli amini walio kuja nayo Mitume, na wakatenda walio wausia, na wakajitenga na alio yaharimisha Mwenyezi Mungu, tungeli wapa baraka nyingi zitokazo mbinguni na kwenye ardhi, kama mvua, na mimea, na matunda, na wanyama, na riziki, na amani na kusalimika na misiba. Lakini wao wakapinga na wakawakadhibisha Mitume. Basi tukawapatiliza kwa adhabu nao wamelala, kwa sababu ya ukafiri na maasi waliyo yazua. Basi huko kushikwa waliko shikwa kwa adhabu ni matokeo ya lazima kuwa kwa ajili ya maovu waliyo yachuma, na yawe kuwa ni somo kwa walio kama wao ikiwa wanayatia akilini!

97 Je, watu wa hii miji walio letewa wito wa Manabii wao na wasiwaamini, wamejiaminisha kuwa adhabu yetu haitawafika nao wamezama katika usingizi wao?

98 Je, watu hawa wameghafilika na wamejiaminisha kuwa adhabu haitawajia mchana kweupe na jua linawaka, nao wameshughulikia mambo yasiyo na faida nao?

99 Je, hawajui mwendo wa Mwenyezi Mungu anavyo kwenda nao wanao kanusha, hata wakajitumainisha kuwa haitawafikia adhabu usiku au mchana? Naye, huipeleka kwa mpango wake wasio uona watu. Hakika hawawi wajinga wa mpango na mwendo wa Mwenyezi Mungu katika kuadhibu ila wale wanao kanusha, wenye kuzikhasiri nafsi zao kwa kutozinduka katika mambo yaliyo khusu kufanikiwa kwao.

100 Je, hawajui mwendo wa Mwenyezi Mungu kwa kaumu zilizo kwisha pita kabla yao, na kuwa shani yetu kwao ni kama ilivyo kuwa kwa walio watangulia? Na kwamba wao lazima wafuate tuyatakayo. Tukitaka kuwaadhibu kwa sababu ya madhambi yao tutawapatiliza kama tulivyo wapatiliza walio kama wao. Nasi tunatia muhuri nyoyo zao kwa kuwa zimeharibika bila ya kiasi, mpaka ikafika ukomo kuwa hazipokei tena uwongofu. Kwa muhuri huo imekuwa hawasikii hikima wala nasiha, kwa msikio wa kufahamu na kuwaidhika.

101 Hiyo ni miji iliyo dumu karne nyingi, na imepitwa na muda mrefu katika taarikhi yao. Tunakusimulia hivi sasa baadhi ya khabari zao zenye somo la kuzingatiwa. Na watu wa miji hiyo walifikiwa na Mitume wao kwa Ishara zilizo wazi zenye kuonyesha ukweli wa wito wao. Lakini haikuwa shani yao kuamini baada ya kuja hizo Ishara zilizo wazi, kwa sababu ya mtindo wao wa kuwakanusha wasemao kweli. Basi wakawakadhibisha Mitume wao, wala hawakuongoka! Basi ni hivyo Mwenyezi Mungu huweka kizuizi juu ya nyoyo na akili za makafiri, ikafichika kwao Njia ya Haki, na wakajitenga nayo.

102. Wala hatukuwakuta wengi wa watu hao kuwa ni wenye kutimiza ahadi kwa Imani tulio wausia kwa ndimi za Mitume, na yanayo tambuliwa na akili na nadhari nzuri. Na mwendo ulio thibiti kwao ni vile kuselelea katika upotofu na kwenda kinyume na kila ahadi.

wake. Nao wakazikataa. Basi tazama ulikuwaje mwisho wa waharibifu.¹⁰³

104. Na Musa alisema: Ewe Firauni! Hakika mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote.¹⁰⁴

105. Inafaa nisiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila lilio la Haki. Nami hakika nimekujieni na dalili waziwazi kutokana na Mola Mlezi wenu. Basi waache Wana wa Israili wende nami.¹⁰⁵

106. Akasema Firauni: Ikiwa umekuja na Ishara, basi ilete ukiwa ni katika wasemao kweli.¹⁰⁶

107. Basi akaitupa fimbo yake, na mara ikawa nyoka dhaahiri.¹⁰⁷

108. Na akatoa mkono wake, mara ukawa mweupe kwa watazamao.¹⁰⁸

109. Wakasema waheshimiwa wa kaumu ya Firauni: Hakika huyo ni mchawi mjuzi.¹⁰⁹

110. Anataka kukutoeni katika nchi yenu. Basi mnatoa shauri gani?¹¹⁰

111. Wakasema: Mwache kidogo yeye na nduguye, na watume mijini wakusanyao,¹¹¹

112. Wakuletee kila mchawi mjuzi.¹¹²

113. Wakaja wachawi kwa Firauni, wakasema: Hakika tutapata ujira ikiwa tutashinda.¹¹³

114. Akasema: Naam! Nanyi bila ya shaka mtakuwa katika wa karibu nami.¹¹⁴

103 Tena baada ya Mitume hao tulimtuma Musa a.s. Naye akaja na dalili zenye kuonyesha ukweli wa anayo yafikisha kutokana nasi kumpelekea Firauni na kaumu yake. Musa akaufikisha wito wa Mola wake Mlezi, na akawaonyesha Ishara ya Mwenyezi Mungu. Nao wakadhulumu nafsi zao na watu wao kwa kuzikataa kwa kiburi na upinzani tu! Basi wakastahiki adhabu kali kutokana na Mwenyezi Mungu, na hivyo ukawa mwisho wa mambo yao! Basi ewe Nabii! Angalia vyema mwisho wa mafisadi katika ardhi.

104 Musa akasema: Ewe Firauni! Hakika mimi nimetumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote, Mwenye mamlaka juu ya mambo yao yote, ili nikufikishieni wito wake, na nikuiteni muifuatae Sharia yake.

105 Na mimi pupa yangu ni kumsema kweli Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na nimekujieni na Ishara yenye shani kubwa, yenye hoja iliyo dhaahiri katika kubainisha Haki niliyo kuja nayo. Basi waachilie waje nami Wana wa Israili, na uwatoe kwenye utumwa wa kahari yako, wende nami kwenye nchi nyengine isiyokuwa yako, na huko wapate kumuabudu Mola Mlezi wao na wako.

106 Firauni akamwambia Musa: Ikiwa umekuja na Ishara (muujiza) kutokana na huyo aliye kutuma, basi nionyeshe kama wewe ni katika watu wakweli wanalo lishika neno la haki.

107 Kiasi ya Musa kuitupa fimbo aliyokuwa nayo mkononi mwake wa kulia mbele ya Firauni, mara hiyo fimbo ikawa nyoka khasa dhaahiri, anakwenda mbio huku na huku, kwa nguvu zinazo onyesha kuwa ana uhai timamu.

108 Akautoa mkono wake kutoka mfukoni mwake, na hapo hapo ukawa mweupe safi kabisa ukimeremeta katika macho ya wanao angalia!

109 Musa alipo ionyesha Ishara ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, zilitibuka roho za wapambe wa Firauni na waheshimiwa wa kaumu yake, wakasema katika kujipendekeza kwa Firauni na kumtetea: Hakika huyu ni bingwa katika ilimu ya uchawi, wala hii si Ishara itokayo kwa Mwenyezi Mungu!!

110 Na yeye ameelekeza lengo lake akupokonyeni ufalme wenu, na akutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake na yatayo tokea hapo kwa kuwavutia watu wamili na wamfuatae. Basi tazameni, mnaamrisha njia gani ya kutokana naye huyu?

111 Wakasema: Akhishisha kukata shauri juu yake na nduguye huyu anaye msaidia katika wito wake, na watume watu katika askari wako wende katika miji ya ufalme wako wawakusanye walio mafundi katika ilimu ya uchawi.

112 Wakuletee kila mwanachuoni wa ilimu za uchawi. Na wao watakufichulia nini khasa hakika ya aliyokuja nayo Musa, asije akafitnika yeyote.

113 Basi wakaja kwa Firauni wachawi walio kusanywa na askari wake. Nao wakasema: Hapana shaka nasi tutapata malipo makubwa yanayo lingana na hili linalo takikana kwetu, ikiwa sisi tutamshinda Musa.

114 Haraka haraka Firauni akawajibu kwa walitakalo: Naam! Hapana shaka mtapata malipo makubwa. Na hapana shaka juu ya hayo nyinyi mtakuwa watu wenye cheo kwangu.

- 115.** Wakasema: Ewe Musa! Je, utatupa wewe, au tutakuwa sisi tutao tupa?¹¹⁵
- 116.** Akasema: Tupeni! Basi walipo tupa waliyazuga macho ya watu na wakawatia khofu, na wakaleta uchawi mkubwa.¹¹⁶
- 117.** Nasi tukamfunulia Musa kumwambia: Tupa fimbo yako. Mara ikavimeza vyote vile walivyo vibuni.¹¹⁷
- 118.** Kweli ikathibiti na yakabat' ilika waliyo kuwa wakiyatenda.¹¹⁸
- 119.** Kwa hivyo walishindwa hapo, na wakageuka kuwa wadogo.¹¹⁹
- 120.** Na wachawi wakapoomoka wakisujudu.¹²⁰
- 121.** Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa viumbe vyote,¹²¹
- 122.** Mola Mlezi wa Musa na Haarun.¹²²
- 123.** Akasema Firauni: Mmemuamini kabla sijakupeni idhini? Hizi ni njama mlizo panga mjini mpate kuwatoa wenyewe. Lakini karibu mtajua!¹²³
- 124.** Lazima nitakata mikono yenu na miguu yenu mbali mbali. Kisha nitakutundikeni misalabani.¹²⁴
- 125.** Wakasema: Sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi.¹²⁵
- 126.** Nawe hukuudhika nasi ila kwa kuwa tumeziamini Ishara za Mola Mlezi wetu zilipo tujia. Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie uvumilivu na utufishe hali ni Waislamu.¹²⁶

115 Kisha wachawi wakamgeukia Musa, baada ya Firauni kuwaahidi alivyo waahidi, na wao wakaonyesha wana imani na nafsi zao na kujitayarisha kwao kwa uchawi wao katika uwanja wa mapambano. Wakamwambia: Ama utupe ulicho nacho kwanza, au sisi tuwe wenye kutupa tulicho nacho.

116 Musa akwajibu jawabu ya mwenye imani ya kushinda, akionyesha kutowabali: Tupeni nyinyi kwanza hicho mnacho tupa. Walipo tupa kila mmoja wao, navyo ni kamba na fimbo, macho ya watu yalizugwa, na ikawapitikia kuwa walicho kifanya kile ni hakika kweli. Na hali haikuwa ila ni kiini macho tu. Mambo yale yaliwatisha watu, na nyoyo zao zikaingia khofu na kitisho. Kwani wachawi wale waliwaletea watu uchawi unao onekana ni mkubwa, na athari yake katika macho yao ni kubwa!

117 Mwenyezi Mungu akaitoa amri yake kumpelekea Musa: Tupa fimbo yako. Sasa umekwisha fika wakati wake. Akaitupa kama alivyo amrisha. Mara hiyo fimbo ikaingia kuvimeza vile vizushi vyao walivyo zua na kubuni!

118 Basi Haki ikathibiti na kudhihiri upande wa Musa a.s. na ukabwatika udanganyifu wa wachawi.

119 Firauni na waheshimiwa wake wakashindwa katika ule mkutano mkubwa, na wakawa madhalili mbele ya watu wote kwa masabu yaliyo wapata, nayo ni kuvunjika moyo na kukata tamaa.

120 Haya ni mambo yaliyo wafika Firauni na waheshimiwa wake. Ama wale wachawi Haki ilianguza kwao, na wakaanguka kwa kumsujudia Mwenyezi Mungu nao wanainyenyekea Haki..

121 Huku wakisema hao wachawi walio tubia: Tumemuamini Muumba wa viumbe vyote, Mwenye kumiliki na kuendesha mambo yao yote.

122 Hakika huyo ndiye Mungu anaye itakidiwa na kuaminiwa na Musa na Haarun.

123 Jambo hili lilimtisha Firauni na ikafoka ghadhabu yake, akasema: Hivyo nyinyi memmuamini na kumsadiki Mola Mlezi wa Musa na Haarun kabla sijakupeni ruhusa mimi? Hakika hapa pana kijambo mmekizua nyinyi na Musa na Haarun kwa kuwafikiana. Na haya si chochote ila ni vitimbi mlivyo vipanga katika mji wa Misri mpate kuwatoa wenyewe kwa hila yenu. Basi ngojeni, mtaiona adhabu itayo kushukieni kuwa ndio jaza yenu kwa kumfuata Musa na Haarun, na ndio adabu yenu kwa hivi vitimbi vyenu na khadaa!

124 Na ninakuapieni kuwa nitakuteseni vikali, na nitakukateni mikono yenu na miguu yenu mbali mbali, nitakata mkono wa upande mmoja na mguu wa upande wa pili, kisha nitakutundikeni misalabani, kila mmoja wenu, nanyi mmo katika hali hiyo, ili muwe ni zingatia kwa anaye jifikiria kutufanyia vitimbi, au kutaka kuufanyia uasi utawala wetu!

125 Nao hawakuibali kauli yake wala vitisho vyake, kwa kuwa Imani ilikwisha saki ndani ya nyoyo zao. Wakamwambia: Hakika sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi. Kwa hivyo tunaneemeka katika rehema yake na bora ya malipo yake.

126 Na wewe hutuchukii na kutuadhibu ila kwa kuwa tumemsadiki Musa, na tumezikubali zilipo tujia

127. Wakasema waheshimiwa wa kaumu ya Firauni: Unamuacha Musa na watu wake walete uharibifu katika nchi na wakuache wewe na miungu yako? Akasema: Tutawauwa wavulana wao, na tutawaacha hai wanawake wao. Na bila ya shaka sisi ni wenye nguvu juu yao.¹²⁷

128. Musa akawaambia watu wake: Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu, na subirini. Hakika ardhi ni ya Mwenyezi Mungu. Naye humrithisha amtakaye katika waja wake. Na mwisho ni wa wachamngu.¹²⁸

129. Wakasema: Tumeudhiwa kabla hujatufikia, na baada ya wewe kutujia! Musa akasema: Huenda Mola wenu Mlezi akamhiliki adui wenu, na akakufanyeni nyinyi ndio wa kufuatia kushika nchi, ili atazame mtavyo kuja tenda nyinyi.¹²⁹

130. Na hakika tuliwaadhibu watu wa Firauni kwa miyaka (ya ukame) na kwa upungufu wa mazao, ili wapate kukumbuka.¹³⁰

131. Likiwafika jema wakisema: Haya ni haki yetu. Na likiwafika ovu husema: Musa na walio pamoja naye ni wakorofi. Hakika ukorofi wao huo unao wafikia unatoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui.¹³¹

Ishara za Mola wetu Mlezi zililo wazi, zenye kuonyesha Haki! Kisha wakamuelekea Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu, wakisema: Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie subira kubwa, itupe nguvu kuhimili shida zote; na utufishe katika Uislamu bila ya kuteseka kwa anayo tuahidi Firauni.

127 Baada ya Firauni na watu wake kuona waliyo yaona, katika vile kudhihiri mambo ya Musa na nguvu za ushindi wake, na wachawi wakamuamini, walisema wakuu wa kaumu yake: Unamuacha Musa na watu wake wawe huru katika amani, ili mwisho wao wawafisidi kaumu yako dhidi yako katika nchi ya Misri kwa kuwatia katika dini yao, na wakuache wewe na miungu yako bila ya wao kujali? Hapo watu wa Misri watakuona wewe na hiyo miungu kuwa mmeshindwa. Firauni akasema kuwajibu: Tutawauwa watoto wao wa kiume wa watu hawa, kila anaye zaliwa; na tutawabakisha wa kike wawe hai, ili wasiwe na nguvu, kama tulivyo fanya zamani. Na sisi tuko juu yao kwa kuwashinda na kwa utawala, na kuwafanyia kahari.

128 Na hapo Musa aliona kama dalili za huzuni katika watu wake, basi akawatia nguvu katika azma yao. Akawaambia: Mtakeni Mwenyezi Mungu msaada na kukuungeni mkono. Na kuweni imara, wala msifazaike. Kwani ardhi yote imo katika nguvu za uwezo wa Mwenyezi Mungu na ufalme wake. Humrithisha amtakaye katika waja wake, wala si ya Firauni. Na mwisho mwema wataupata wale wanao mcha Mwenyezi Mungu kwa kushikamana naye na kuzikamata hukumu zake.

129 Wakasema wale watu kwa huzuni na unyonge: Sisi tulipata maudhi zamani kutoka kwa Firauni kabla hujatujia, na hivi sasa tena baada ya kuja kwako. Musa akawafungulia mlango wa matarajio mema kwa kuwaambia: Hakika linalo tarajiwa kwa fadhila za Mola wenu Mlezi ni kumteketeza adui yenu, aliye kufanyeni watumwa na akakuteseni kwa dhulma yake, na akujaalieni nyinyi ndio wa kuimiliki ardhi aliyo kuahidini. Yeye *Subhanahu*, Aliye takasika, anayajua mnayo yatenda baada ya kukuwekeni huku. Je, mtaishukuru neema au mtaikufuru? Na mtatenda mema katika nchi au mtafanya fisadi? Hayo ili apate kukulipeni duniani na Akhera kwa mujibu wa mtendayo.

130 Na hakika Sisi tuliwaadhibu Firauni na watu wake kwa ukame, na dhiki ya maisha, na upungufu wa matunda na mazao na miti, kwa kutaraji kuwa watazindukana wautambue unyonge wao, na kushindwa ufalme wao wa jeuri mbele ya nguvu za Mwenyezi Mungu, wapate kuwaidhika na waache kuwadhulumu Wana wa Israili, na wauitikie wito wa Musa a.s. Kwani mtindo wa shida ni kuzuia kujidanganya, na kutengeza tabia, na kuzielekeza nafsi ziikubali Haki, na kumridhi Mola Mlezi wa viumbe vyote, na kumnyenyekea Yeye tu, si mwenginewe.

131 Lakini tabia ya Firauni na wasaidizi wake ni kuto thibiti juu ya Haki. Wepesi kurejea kwenye khiana na uasi. Hao ni watu wa kigeugeu! Ikiwajia kutoonoka na neema - na mara nyingi huwa hivyo - wao wakisema: Sisi tunastahiki haya tuliyo nayo kuwapita watu wengineo! Na likiwasibu la kuwaudhi, kama ukame, au tauni, au msiba wa miili au riziki, wakiona yamewapata hayo kwa ukorofi wa Musa na walio pamoja naye. Na wanaghafilika kuwa dhulma zao, na fisadi zao ndizo zilizo pelekea kuja hayo yanayo wapata! Basi na watanabahi, na wajue kuwa ujuzi wa ukorofi wao uko kwa Mwenyezi Mungu. Yeye

- 132.** Na wakisema: Hata ukituletea Ishara yoyote kutuzuga hatuto kuamini.¹³²
- 133.** Basi tukawapelekea tufani, na nzige, na chawa, na vyura, na damu, kuwa ni Ishara mbali mbali. Nao wakapanda kiburi, na wakawa watu wakosefu.¹³³
- 134.** Na ilipo waangukia adhabu wakasema: Ewe Musa! Tuombe kwa Mola wako Mlezi kwa aliyo kuahidi. Ukituondolea adhabu hii hapana shaka tutakuamini, na tutawaachilia Wana wa Israili wende nawe.¹³⁴
- 135.** Lakini tukiwaondolea adhabu mpaka muda fulani wao waufikie, mara wakivunja ahadi yao.¹³⁵
- 136.** Basi tuliwapatiliza, tuka- wazamisha baharini kwa sababu walizikanusha Ishara zetu, na wakaghafilika nazo.¹³⁶
- 137.** Na tukawarithisha watu walio kuwa wanadharauliwa mashariki na magharibi ya ardhi tuliyo ibariki. Na likatimia neno jema la Mola Mlezi wako juu ya Wana wa Israili, kwa vile walivyo subiri. Na tukayaangamiza aliyo kuwa akiyafanya Firauni na kaumu yake, na waliyo kuwa wakijajenga.¹³⁷
- 138.** Na tukawavusha bahari Wana wa Israili, wakafika kwa watu wanao abudu masanamu yao. Wakasema: Ewe Musa! Hebu tufanyie na sisi miungu kama hawa walivyo kuwa na miungu. Musa akasema: Hakika nyinyi ni watu msio jua kitu.¹³⁸

ndiye anaye wapatiliza kwa sababu ya vitendo vyao viovu. Yeye ndiye anaye wapelekea hayo yanao waudhi, wala si Musa na alio nao. Lakini wengi wao hawajui Hakika ambayo haina shaka.

132 Na kwa hii fikra mbovu waliyo nayo wakaendelea na upinzani. Walisema walipo ona miujiza ya Musa: Wewe hata ukituletea kila namna ya Ishara zinazo onyesha ukweli wa wito wako, ili kutuachisha dini yetu, na tusiwafanye watumwa watu wako, sisi hatukusadiki wala hatukufuati.

133 Basi Mwenyezi Mungu aliwateremshia masaibu na balaa zaidi, kama tufani lilio funika mwahala mwao, na nzige walio kula kila mmea na mti ulio bakia, na chawa, yaani vijidudu vinavyo haribu matunda na kuteketeza wanyama na mimea. na vyura vilivyo enea vikafanya maisha yao dhiki, na vikachafua kila pahala, na damu iliyo sabibisha maradhi mengi, kama kupasuka mishipa ya damu katika mwili, na damu inayo najisisha kila pahala ikasabibisha presha, au kupasuka ikaleta kiharusi na kupooza, na kutokwa na mkojo wa damu kwa sababu ya kichocho na mfano wake, au ikawa inachanganyika na maji yao wanayo hitajia kunywa au kupikia. Mwenyezi Mungu aliwapatiliza na Ishara hizi zote zilizo wazi! Nao wasiathirike, nyoyo zao zikabaki kuwa ngumu, na wenye kutakabari hawataki Imani wala kurejea kwenye Haki. Walikuwa watu walio bobea kwenye madhambi na ukosefu, kama ilivyo ada yao

134 Katika kuzidi kigeugeu chao kama zinavyo badilika sababu, walikuwa kila ikiwashukia namna yoyote ya adhabu wakisema kwa shida na machungu yanayo wapata: Ewe Musa! Tuombe kwa Mola Mlezi wako, kwa vile alivyo kuahidi kuwa ukimwomba atakupa miujiza na atakuitikia dua, atuondolee adhabu hii. Na sisi tunakuapia kuwa ukituondolea basi bila ya shaka tutakuitikia na tutawaachilia wende nawe Wana wa Israili kama ulivyo taka!

135 Tulipo waondolea adhabu kila mara kwa muda wao mpaka mwisho wake ukisha huivunja ahadi yao, na huenda kinyume na kiapo chao, na hurejea yale yale waliyo kuwa nayo. Kwao wao hayo majaribio ya kuwaachisha maovu hayakuleta faida!

136 Tuliwateremshia nakama yetu. Tukawazamisha baharini kwa sababu ya kushikilia kwao kukanusha Ishara zetu, na hadi ya kutoyabali mafunzo ya Imani na ut'iifu yaliyomo katika hizo Ishara.

137 Tukawapa watu ambao walikuwa wakidharauliwa katika Misri, nao ni Wana wa Israili, ardhi alio ipa baraka Mwenyezi Mungu kwa kuifanya ina rutba na kheri nyingi, tangu mashariki mpaka magharibi yake. Neno jema la Mwenyezi Mungu likatekelezwa kwa ukamilifu, na pia ahadi yake ya ushindi kwa Wana wa Israili, kwa sababu ya kuvumilia kwao dhiki. Na tukayateketeza majumba ya fakhari, na kila majenzi, na chanja za mimea ya kutambaa, na bustani, na pandio za mizabibu, waliyo kuwa wakisimamisha na kujenga akina Firauni na watu wake! Hiyo ndiyo shani ya Mwenyezi Mungu, na ametimiza kweli ahadi yake kwa Wana wa Israili.

138 Wana wa Israili wakaiwuka bahari kwa uangalizi wetu, na kuwaunga mkono na kuwafanyia mepesi mambo yao. Baada ya kwisha vuka waliwakuta kaumu wameshika ibada ya masanamu. Walipoona hivi

139. Hakika haya waliyo nayo watu hawa yatakuja angamia, na hayo waliyo kuwa wakiyafanya yamepotea bure.¹³⁹

140. Akasema: Je, nikutafutieni mungu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na Yeye ndiye aliye kufadhilisheni juu ya viumbe vyote?¹⁴⁰

141. Na pale tulipo kuokoeni kwa watu wa Firauni walio kupeni adhabu za mwisho wa uovu. Wakiwauwa wavulana wenu, na wakawaacha hai wanawake wenu. Na katika hayo yalikuwa majaribio makubwa kutokana na Mola wenu Mlezi.¹⁴¹

142. Tulimuahidi Musa masiku thalathini na tukayatimiza kwa kumi; ikatimia miadi ya Mola wake Mlezi masiku arubaini. Na Musa akamwambia nduguye Haarun: Shika mahala pangu kwa watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu.¹⁴²

143. Na alipo kuja Musa kwenye miadi yetu, na Mola wake Mlezi akamsemeza, alisema: Mola wangu Mlezi! Nionyeshe nikutazame. Mwenyezi Mungu akasema: Hutoni. Lakini utazame huo mlima. Ukibaki pahala pake basi utaniona. Basi alipo jionyesha Mola Mlezi wake kwa mlima, aliufanya uvurugike, na Musa akaanguka chini amezimia. Alipo zindukana alisema: *Subhanaka*, Umetakasika! Natubu kwako, na mimi ni wa kwanza wa Waumini.¹⁴³

144. (Mwenyezi Mungu) akasema: Ewe Musa! Mimi nimekuteuwa wende kwa watu na Ujumbe wangu na maneno yangu. Basi chukua niliyo kupa na uwe katika wanao

yale waliyo kuwa wameyazoea kuwaona Wamisri wakiabudu masanamu yaliwaghibu, wakamtaka Musa awafanyie nao masanamu wayaabudu, kama ilivyo kuwa wale kaumu wana masanamu yao wanayo yaabudu! Hapo hapo Musa a.s. aliwatahayarisha na kuwakanya, akasema: Hakika nyinyi ni watu wapumbavu, msio na akili! Hamjui ibada ya Haki, wala hamumjui Mungu anaye stahiki kuabudiwa!

139 Hawa mnao waona wanaabudu masanamu, hapana shaka haya walio nayo ni yenye kuangamia, na hii dini waliyo nayo ni potovu, bure bilashi. Na a'mali zao ni zenye kupotea, wala hazibaki.

140 Je, nikutafutieni wa kuabudiwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe vyote, na Yeye ndiye aliye kupeni fadhila, na akakupeni neema asio pata kupewa mwengine asiye kuwa nyinyi katika zama zenu?

141 Kumbukeni alipo kuvuoni Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa uangelizi wake na watu wa Firauni, walio kuwa wakikuadhibuni ukomo wa adhabu, wakikudhalilisheni muwatumikie katika kazi ngumu, wala hawakuoneeni huruma kama wanyama, wakiuwa wavulana wenu na wakiwabakisha wasichana ili mzidi kudhoofika kwa wingi wa wanawake! Na katika adhabu za Firauni zilizo kushukieni, na kukuvuoni nazo, pana mtihani mkubwa wa Mola wenu Mlezi, wala hapana mfano wake.

142 Tulimuahidi Musa tutazungumza naye na tutampa Taurati baada ya kutimia masiku (wingi wa "usiku") thalathini ya yeye kuabudu. Na tukauongeza muda huo kwa masiku kumi, kutimiza ibada. Yakawa masiku arubaini. Musa akamwambia nduguye Haarun alipo kuwa anakwenda kuzungumza na Mwenyezi Mungu: Kuwa badala yangu kwa hawa watu wangu. Na watengenezee mambo yao yanayo hitajia kutengenezwa. Na tahadhari na kufuata njia ya mafisadi. (Angalia: Kwa Kiswahili safi, "Masiku" ni wingi wa "Usiku". Ama wingi wa "Siku" ni "Siku" vile vile kama ilivyo katika aghlabu ya maneno mengine yanayoanzia "S", kama Saa, Sanda, Sahani, Sabuni, Safari, Sufuria n.k.)

143 Na alipo kuja Musa kuzungumza nasi, na Mola Mlezi wake akanena naye kwa maneno ambayo siyo kama kusema kwetu, Musa alisema: Ewe Mola Mlezi wangu! Nionyeshe dhati yako na unidhihirikie, nipate kukutazama nizidi utukufu. Mwenyezi Mungu akasema: Huwezi kuniona. Kisha *Subhanahu*, Aliye takasika alitaka kumkainisha kuwa hawezi kumwona, akamwambia: Walakini utazame huo mlima ambao una nguvu kuliko wewe. Ukithibiti pahala ulipo wakati wa kudhihiri kwangu, basi utaniona nikijidhihirisha kwako. Basi Mola wake Mlezi alipo jionyesha kwa huo mlima kwa njia inayo wafikiana naye Mtukufu, mlima ulivurugika ukawa sawa sawa na ardhi. Musa akaanguka, kazimia kwa kitisho alichokiona. Alipo zindukana kutokana na kuzimia kwake alisema: Nakutakasa mtakaso mkuu na kuonekana kwako duniani! Hakika mimi ninatubu kwako kuja kukutaka kitu bila ya ruhusa yako. Na mimi ni wa mwanzo katika zama zangu wa wanao amini utukufu wako na ubora wako.

shukuru.¹⁴⁴

145. Na tukamuandikia katika mbao kila kitu, mawaidha na maelezo ya mambo yote. (Tukamwambia): Basi yashike kwa nguvu na uwaamrishe watu wako wayashike kwa ubora wake. Nami nitakuonyesheni makaazi ya wapotofu.¹⁴⁵

146. Nitawatenga na Ishara zangu wale wanao fanya kiburi katika nchi bila ya haki. Na wao wakiona kila Ishara hawaiamini. Wakiiona njia ya uwongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia; lakini wakiiona njia ya upotofu wanaishika kuwa ndiyo njia. Hayo ni kwa sababu wamezikanusha Ishara zetu, na wameghafilika nazo.¹⁴⁶

147. Na walio zikanusha Ishara zetu na mkutano wa Akhera a'mali zao zimeharibika. Kwani watalipwa ila kwa yale waliyo kuwa wakiyatenda?¹⁴⁷

148. Na baada yake walimfanya ndama kutokana na mapambo yao (kumuabudu), kiwiliwili tu kilicho kuwa na sauti. Hivyo, hawakuona kuwa hawasemezi wala hawaongoi njia? Wakamuabudu, na wakawa wenye kudhulumu.¹⁴⁸

149. Na walipo juta na wakaona ya kwamba wamekwisha potea, walisema: Ikiwa Mola wetu Mlezi hakutuhemu na akatusamehe, bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa walio khasiri.¹⁴⁹

150. Na alipo rudi Musa kwa watu wake, naye amekasirika na kuhuzunika, alisema: Ni maovu yalioje mlio nifanyia nyuma yangu! Je, mmeitangulia amri ya Mola wenu Mlezi? Na akaziweka chini zile mbao, na akamkamata kichwa ndugu yake akimvutia kwake. (Haarun) akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Hakika hawa watu

144 Mwenyezi Mungu alipo mzuilia Musa asimwone, akaingia kumhisabia neema zake ili amliwaze kwa vile kumkatalia, akamwambia: Ewe Musa! Mimi nimekufadhilisha, na nimekuteua kuliko watu wote wa zama zako, ili ufikishe vitabu vya Taurati, na kwa kusema nawe bila ya kuwapo mtu kati. Basi yashike hayo niliyo kukufadhili, na unishukuru kama wafanyavyo wenye kushukuru, wanao kadiri neema.

145 Na tulimbainishia Musa katika zile mbao za Taurati kila kitu kilicho khusu mawaidha na hukumu zilizo elezwa mbali mbali, wanazo hitajia watu duniani na Akhera. Na tukamwambia: Zishike hizi mbao baraabara na kwa kuazimia. Na waamrishe watu wako washike yaliyo bora humo, kama kusamehe badala ya kulipiza kisasi, na kuachilia badala ya kungojea, na kulegeza badala ya kukaza. Enyi kaumu ya Musa! Nitakuonyesheni katika vitabu vyenu makaazi ya wale wanao asi amri za Mwenyezi Mungu, na watavyo angamia, ili mpate kuzingatia. Basi msende kinyume yakakusibuni yalio wasibu hao waasi.

146 Hao walio majeuji na wakapanda kiburi katika ardhi wakakataa kukubali yaliyo sawa bila ya haki, nitawazuia wasiweze kuzingatia dalili za uwezo wangu ziliomo katika nafsi za watu na jiha zote. Watu hawa hata wakiona kila Ishara inayo thibitisha ukweli wa Mitume wetu hawaisadiki. Na wakiiona njia ya uwongofu hawaipiti, na wakiiona njia ya upotofu ndio wanaipita! Hayo yanatokea kwao kwa sababu wamezikanusha Ishara zetu zililo teremshwa, na wameghafilika na kuongoka kwazo.

147 Na walio zikanusha Ishara zetu zililo teremshwa juu ya Mitume wetu kwa ajili ya uwongofu, na wakakanusha kukutana nasi Siku ya Kiyama, wakakataa kufufuliwa na kulipwa, vitendo vyao walivyo kuwa wakitarajia viwafae vitapotelea mbali. Hawatokuta ila malipo ya kufu na maasi waliyo endelea nayo kuyatenda.

148 Na baada ya Musa kwenda kwenye mlima kusema na Mola Mlezi wake, kaumu yake walichukua vyombo vyao vya kujipamba wakatengeneza Sura ya ndama, asiye na akili wala hatambui kitu. Lakini akitoa sauti mfano wa sauti ya ng'ombe, kwa namna walivyo muunda na ukipita upepo ndani yake. Na aliye waundia ni Saamiryu (Msamaria). Naye akawaamrisha wamuabudu! Upumbavu gani huu wa akili zao! Hivyo wao walipo mfanya ndiye mungu wakamuabudu, hawakuona kuwa hawasemezi, wala hawezi kuwaongoa wafuate njia iliyo sawa? Hakika hawa wamejidhulumu nafsi zao kwa kitendo hichi kiovu.

149 Walipo tambua kuteleza kwao, na makaso yao, wakababaika, na wakajuta majuto makubwa kwa kumfanya ndama ndiye mungu. Makosa yao yakabainika wazi, wakasema: Wallahi! Ikiwa Mola wetu Mlezi hakutusamehe hakika tutakuwa miongoni walio khasiri khasara iliyo dhaahiri; kwa vile kuabudu kisicho faa kuabudiwa.

wamenidharau, na wakakaribia kuniuwa. Basi usiwafurahishe maadui juu yangu, wala usinifanye pamoja na watu madhaalimu.¹⁵⁰

151. (Musa) akasema: Mola Mlezi wangu! Nisamehe mimi na ndugu yangu, na ututie katika rehema yako. Nawe ni Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.¹⁵¹

152. Hakika wale walio muabudu ndama, itawapata ghadhabu ya Mola wao Mlezi na madhila katika maisha ya dunia. Na hivi ndivyo tunavyo walipa wazushi.¹⁵²

153. Na walio tenda maovu, kisha wakatubia baada yake na wakaamini, hapana shaka kuwa Mola Mlezi wako baada ya hayo ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.¹⁵³

154. Na Musa ilipo mtulia ghadhabu aliziokota zile mbao. Na katika maandiko yake mna uwongofu na rehema kwa wanao mwogopa Mola wao Mlezi.¹⁵⁴

155. Na Musa akawateuwa watu sabiini katika kaumu yake kwa miadi yetu. Na ulipo fika mtetemeko mkubwa alisema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ungeli taka ungelihali wawiliki wao na mimi zamani! Unatuhiliki kwa waliyo yafanya wajinga katika sisi? Haya si chochote ila ni mtihani wako, umpoteze umtakaye na umhidi umtakaye. Wewe ndiye Rafiki Mlinzi wetu. Basi tughufirie na uturehemu. Na Wewe ndiye mbora wa kughufiria.¹⁵⁵

150 Na Musa alipo rejea kutoka kuzungumza na Mola Mlezi wake kuja kwa watu wake, naye kakasirika nao kwa vile walivyo muabudu ndama, na amehuzunika kwa kuwa Mwenyezi Mungu amewatia mtihanini - kwani Mwenyezi Mungu alikwisha mpa khabari ya yale kabla hajarejea - aliwaambia: Kitendo gani kiovu hichi mli cho kitenda baada ya kuondoka kwangu! Mmetangulia kwa kumuabudu ndama msifuate amri ya Mola wenu Mlezi kuwa mningojee, na mkawa hamkuishika ahadi yangu mpaka nikakuleteeni Taurati? Akaziweka zile mbao, na akamuelekea nduguye kwa huzuni kubwa kwa yale aliyo yaona kwa kaumu yake. Akaingia kumvuta ndugu yake kwa kichwa akimbururia kwake kwa wingi wa ghadhabu. Haya ni kuwa alidhani kuwa amefanya taksiri hakuwazuia kufanya walio yafanya! Haaran akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Hakika hawa watu walipo fanya waliyo yafanya walinidharau na wakanishinda nguvu. Na wakakaribia kuniuwa kwa kuwa niliwakataza wasimuabudu ndama. Basi usiwafurahishe maadui kwa kunitesa mimi, wala usitakidi kuwa mimi ni mmoja wa wenye kudhulumu, kwani mimi ni mbali nao na dhulma yao. (*Tazama maelezo 7:150*)

151 Musa alisema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nisamehe kwa haya niliyo mfanyia ndugu yangu kabla sijayajua mambo. Na msamehe ndugu yangu ikiwa kakosea katika kushika pahala pangu kwa vizuri. Na tuingize katika eneo la rehema yako, kwani Wewe ndiwe Mwenye rehema nyingi kushinda wote wenye kurehemu.

152 Hakika wale walio endelea kumfanya ndama kuwa mungu, kama Msamaria na wenziwe, itawafika ghadhabu kubwa kutoka kwa Mola wao Mlezi huko Akhera, na uvunjifu mkubwa katika maisha ya duniani. Na mfano wa malipo hayo ndio tunamlipa kila mwenye kumzulia Mwenyezi Mungu uwongo, na akaabudu kinginecho.

153 Na wale walio tenda vitendo vibaya vya ukafiri na kuabudu ndama na maasi mengineyo, kisha wakarejea kwa Mwenyezi Mungu baada ya kutenda hayo, na wakamsadiki, basi hakika Mola wako Mlezi baada ya toba yao, ni Mwenye kuwasitiri, na kuwasamehe kwa hayo waliyo kuwa nayo.

154 Na Musa zilipo muondoka ghadhabu kwa kutoa udhuru nduguye, akazirejea zile mbao alizo ziweka chini akazichukua. Na kwenye hizo mbao umeandikwa uwongofu, na uwongozi, na njia za kupata rehema, kwa wale wanao iogopa ghadhabu ya Mola wao Mlezi.

155 Kisha Mwenyezi Mungu alimuamrisha awalete baadhi ya jamaa katika kaumu yake wawatakie radhi walio muabudu ndama, na akawapa miadi. Musa akawateuwa katika kaumu yake watu sabiini katika wasio muabudu ndama, nao wakawa wanawawakilisha kaumu yao. Akenda nao mpaka kwenye mlima. Na huko wakamwomba Mwenyezi Mungu awaondolee balaa, na akubali toba ya walio muabudu ndama kati yao. Ikawachukua zilzala (tetemeko) kubwa pahala hapo, wakazimia kwa sababu yake. Na hayo kwa kuwa hawakuwaacha kaumu yao walipo abudu ndama, wala hawakuamrisha mema, wala hawakuwakanya maovu! Musa alipoona yale alisema: Ewe Mola wangu Mlezi! Lau ungelihali penda kuwaangamiza ungelihali waangamiza kabla hawajaja hapa kwenye miadi, na ukianiangamiza na mimi pia, ili waone hayo Wana

156. Na utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera. Sisi tumerejea kwako. (Mwenyezi Mungu) akasema: Adhabu yangu nitamsibu nayo nimtakaye. Na rehema yangu imeenea kila kitu. Lakini nitawaandikia khasa wanao mchamngu, na wanao toa Zaka, na wale ambao wanaziamini Ishara zetu,¹⁵⁶

157. Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa.¹⁵⁷

158. Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliye tumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana mungu ila Yeye anaye huisha na anaye fisha. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake asiyejua kusoma na kuandika, ambaye anamuamini Mwenyezi Mungu na maneno yake. Na mfuateni yeye ili mpate kuongoka.¹⁵⁸

159. Na katika kaumu ya Musa lipo kundi linao waongoa watu kwa haki na kwa haki wanafanya uadilifu.¹⁵⁹

160. Na tuliwagawanya katika makabila kumi na mbili, mataifa mbali mbali. Na tulimfunulia Musa walipo muomba maji watu wake kumwambia: Lipige hilo jiwe kwa fimbo yako. Mara zikatibuka humo chemchem kumi na mbili, na kila watu wakajua mahali pao pa kunywea. Na tukawafunika kivuli kwa mawingu, na tukawateremshia Manna na Salwa. Tukawaambia: Kuleni vizuri hivi tulivyo kuruzukuni. Wala hawakutu-

wa Israili wasinituhumu kuwa mimi nimewauwa. Basi ewe Mola Mlezi wangu! Usituhiliki kwa walio yafanya wajinga kati yetu. Kwani hii balaa ya kuabudu ndama haikuwa ila ni majaribio yaliyo toka kwako. Wewe unampoteza unaye taka apotee katika hao wanao ishika njia ya shari, na unawahidi unaye taka ahidike. Wewe ndiye mwenye kusema: Nitawaandikia wenye kujikinga na ukafiri na maasi katika kaumu yako, na akatoa Zaka iliyo faridhiwa, na Mwenye kusamehe madhambi.

156 Na tukadirie hapa duniani maisha mema, na tupate tawfiqi tuweze kut'ii, na Akhera tupate malipo mazuri, na maghfira, na rehema, kwa kuwa sisi hakika tumekwisha rejea kwako na tunatubu kwako. Mola Mlezi wao akawaambia: Adhabu yangu namfikishia nimtakaye katika wasio tubu, na rehema yangu imeenea juu ya kila kitu, na nitawaandikia khasa wale wanao jikinga na ukafiri na maasi katika kaumu yako, na wanao toa Zaka zililo lazimishwa, na wanao sadiki Vitabu vyote vilivyo teremka.

157 Na nawakusudia khasa wanao mfuata Mtume Muhammad, ambaye haandiki wala hasomi, na ambaye wanakuta sifa zake zimeandikwa katika vitabu vyao vya Taurati na Injili. Yeye anawaamrisha kila kheri na anawakataza kila shari. Na anawahalalishia vitu ambavyo tabia inaviona ni vizuri, na anawaharimishia vitu ambavyo tabia inavichukia kwa kuwa vina madhara, kama damu na mzoga. Na anawaondolea mizigo mizito na mikazo iliyo kuwa ikiwabana. Basi wanao usadiki Utume wake, na wakamsaidia, na wakamuunga mkono, na wakamnusuru na maadui zake, na wakaifuata Qur'ani aliyo teremshiwa pamoja naye kama nuru ya uwongofu, hao basi ndio wenye kufuzu, sio wengine ambao hawakumuamini.

158 Ewe Nabii! Waambie watu: Hakika mimi nimetumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote, bila ya farka baina ya Mwaarabu na asiye kuwa Mwaarabu, baina ya mweusi na mweupe. Na Mwenyezi Mungu aliye nituma ni Yeye peke yake ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Huiipitisha amri yake kwa mujibu wa hikima yake. Na hufanya mbinguni na duniani kama anavyo penda. Wala hapana wa kuabudiwa kwa haki ila Yeye. Na Yeye ndiye Mwenye uwezo wa kuhuisha na kufisha, wala hapana mwengine. Basi muaminini Yeye na Mtume wake, huyu Nabii asiye soma wala kuandika. Naye huyu anamuamini Mwenyezi Mungu ambaye anaye kuiteni mumuamini. Na anaamini Vitabu vyake vilivyo teremshwa. Basi mfuateni katika kila afanyalo na asemalo mpate kuongoka na kuongozeka.

159 Na katika kaumu ya Musa wako jamaa walio bakia na Dini iliyo sawa. Wakiwahidi watu kwa Haki aliyo kuja nayo Musa kutoka kwa Mola wake Mlezi, na wakifanya uadilifu pale wanapo pitisha hukumu.

dhulumu Sisi, bali wamejidhulumu wenyewe.¹⁶⁰

161. Na pale walipo ambiwa: Kaeni katika mji huu, na mle humo mpendapo, na semeni: Tufutie dhambi zetu. Na ingieni katika mlango wake kwa unyenyekevu, tupate kukusameheni makosa yenu. Walio wema tutawazidishia.¹⁶¹

162. Lakini walio dhulumu miongoni mwao walibadilisha kauli, sio ile waliyo ambiwa. Basi tukawapelekea adhabu kutoka mbinguni kwa vile walivyo kuwa wakidhulumu.¹⁶²

163. Na waulize khabari za mji ulio kuwa kando ya bahari, wakiivunja Sabato (Jumaamosi ya mapumziko). Samaki walikuwa wakiwajia juu juu siku ya mapumziko yao, na siku zisio kuwa za kupumzika hawakuwa wakiwajia. Kwa namna hiyo tuliwajaribu kwa sababu walikuwa wakifanya upotovu.¹⁶³

164. Na kikundi kati yao walisema: Kwa nini mnawawaidhi watu ambao tangu hapo Mwenyezi Mungu atawateketeza au atawaadhibu adhabu kali? Wakasema: Ili uwe ni udhuru kwa Mola Mlezi wenu, na huenda nao wakamchamngu.¹⁶⁴

165. Basi walipo yasahau waliyo kumbushwa, tuliwaokoa walio kuwa wakikataza maovu, na tukawatesa walio dhulumu kwa adhabu mbaya kwa vile walivyo kuwa wakifanya upotovu.¹⁶⁵

160 Mwenyezi Mungu amezitaja neema zake juu ya kaumu ya Musa. Akafahamisha kuwa aliwafanya makundi thinaashara, na akawafanya mataifa, na kila taifa likawa na mpango wao, ili kuzuia uhasidi na kukhitalifiana. Na walipo taka watu wake maji jangwani, alimfunulia Musa alipige jiwe kwa fimbo yake. Akalipiga, zikatibuka kutoka kwenye hilo jiwe chemchem kumi na mbili kwa idadi ya kabila zao. Kila kabila kati yao ilijua pahala pake makhsusi pa kunywa. Basi haikuwa huyu kumuingilia huyu. Na akajaalia kiwingu chende kuwapa kivuli chake katika jangwa, kuwakinga na mwako wa jua. Akawateremshia Manna, nacho ni chakula kwa Sura kinafanana na mvua ya barafu, na tamu kama asali. Na akateremsha Salwa, naye ni ndege aliye nona. Na akawaambia: Kuleni hivi vinono tulivyo kuruzukuni katika tulivyo kuteremshieni. Lakini walijudhulumu nafsi zao, na wakazikufuru neema hizo, kwa kuzikataa na kutaka nyenginezo. Na Sisi hatukupata madhara kwa udhalimu wao, lakini upungufu wamepata wao.

161 Ewe Nabii! Wakumbushe hao waliopo miongoni mwao katika zama zako - ili iwe ni onyo kwa vile walivyo tenda walio watangulia - wakumbushe kauli yetu tulio waambia hao walio watangulia kwa ulimi wa Musa: Kaeni katika mji wa Baitul Muqaddas (Yerusalemu) baada ya kutoka jangwani. Na kuleni kheri zake kokote humo mtakako, na semeni: Tunakuomba ewe Mola Mlezi wetu, utufutie makosa yetu. Na muingie kwenye lango la mji kwa kuinamisha vichwa kama kurukuu kwa kumnyenyekea Mwenyezi Mungu. Mkiifanya hivyo tutakufutieni dhambi zenu, na tutazidisha thawabu za watendao mema.

162 Lakini waliikhaliifu amri ya Mola wao Mlezi, wakasema kwa udhalimu maneno sio walio ambiwa, kwa kusudi ya kumkejeli Musa. Basi tukawateremshia adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya kuendelea kwao na udhalimu na kukiuka mpaka.

163 Na waulize Mayahudi, kwa kuyachukia walio yafanya wenzao walio watangulia, khabari ya kijiji, nacho ni Elat, kilicho kuwa karibu na bahari. Wakaazi wake walivunja amri ya Mwenyezi Mungu ya kupiga marfuku kuvua samaki siku ya Jumaamosi, kuwa hiyo ni siku ya ibada tu kwao. Na siku hiyo samaki walikuwa wakiwajia vururu juu ya maji. Na siku isiyo kuwa Jumaamosi samaki walikuwa hawaji. Huo ni mtihani wa Mwenyezi Mungu! Na kwa mfano wa mtihani huo, au majaribio hayo yaliyo tajwa, ndio tunawajaribu kwa majaribio mengine kwa sababu ya upotovu wao unao endelea, ili adhihiri mwema na mbaya.

164 Na wakumbushe pia hao Mayahudi pale kikundi cha watu wema katika wenzao walio tangulia, ambao hawakutenda mabaya waliyo yatenda wengineo, walipo waambia wanao wapa mawaidha wale waovu: Kwa sababu gani mnawapa nasaha watu ambao Mwenyezi Mungu atawahiliki, au atawaadhibu adhabu kali Akhera, kwa sababu ya madhambi wanayo yatenda? Wakasema: Tunawapa mawaidha ili tupate udhuru kwa Mola wako Mlezi, tusiwe tumefanya taksiri, na kutaraji huenda wakamchamngu.

165 Walipo yaacha mawaidha waliyo pewa, tukawaokoa na adhabu wale ambao walikuwa wakikataza vitendo viovu, na tukwashika walio dhulumu na wakavuka mipaka na wakakhalifu kwa kuwapa adhabu kali, nayo ni udhalili na shakawa, kwa sababu ya kuendelea kwao kutokana na ut'iifu wa Mwenyezi

166. Walipo jifakharisha katika waliyo kanywa tuliwaambia: Kuweni manyani wa kudharauliwa.¹⁶⁶

167. Na pale alipo tangaza Mola wako Mlezi kwamba hapana shaka atawaletea watu ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya mpaka Siku ya Kiyama. Hakika Mola wako Mlezi ni Mwepesi wa kuadhibu, na bila ya shaka ni Mwenye maghfira, na Mwenye kurehemu.¹⁶⁷

168. Na tuliwafarikisha katika ardhi makundi makundi. Wako kati yao walio wema, na wengine kinyume cha hivyo. Na tukawajaribu kwa mema na mabaya ili wapate kurejea.¹⁶⁸

169. Na wakafuatia baada yao kizazi kibaya walio rithi Kitabu. Wakashika anasa za haya maisha duni, na wakasema: Tutasamehewa! Na ikiwajia tena anasa kama hiyo wataishika pia. Je, hawakufanyiwa agano la Kitabu kuwa wasiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila Haki tu? Nao wamekwisha soma yaliomo humo. Na nyumba ya Akhera ni bora kwa wanao jikinga na maasi. Basi je, hamtii akilini?¹⁶⁹

170. Na wale wanao kishikilia Kitabu, na wakashika Sala - hakika Sisi hatupotezi ujira wa watendao mema.¹⁷⁰

171. Na pale tulipo unyanyua mlima juu yao ukawa kama kwamba ni kiwingu kilicho wafunika, na wakadhani kuwa utawaangukia, (tukawaambia): Kamateni kwa nguvu tuliyo kupeni, na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kumcha Mungu.¹⁷¹

Mungu, Mola Mlezi wao.

166 Walipo zidi kuwa wagumu, na wakaendelea kutobali waliyo katazwa, wala adhabu kali isiwaachishe uovu, tukawafanya kama manyani kwa kuzigeuza nyoyo zao, na kuwaondolea uwezo wa kuifahamu Haki, wakawa mbali na kila kheri.

167 Na wakumbushe pia hao Mayahudi pale alipo wajuvya Mola Mlezi wako wenzao walio watangulia kwa ndimi za Manabii wao: Mwenyezi Mungu atawasalitisha Mayahudi mpaka Siku ya Kiyama adhabu mbaya kabisa kwa sababu ya dhulma yao na upotovu wao. Kwani Mola wako Mlezi ni Mwepesi wa kuwaadhibu watu makafiri, kwani adhabu yake itakuja tu bila ya shaka yoyote. Na kila kijacho kipo karibu, (chambilecho Waarabu). Na Yeye Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu kwa anaye rejea kwake akatubu.

168 Na Sisi tumewagawa makundi makundi duniani. Wamo kati yao walio wema. Na hao ndio walio amini wakenda mwendo ulio sawa. Na wapo miongoni mwao watu wasio sifika kwa wema. Na wote tumewafanyia mitihani kwa kuwapa neema na kuwapa nakama, ili watubu, waache waliyo katazwa.

169 Baada ya hao tulio kwisha wataja na tukawagawa sehemu mbili, walifuatia waovu wakairithi Taurati kutokana na walio watangulia. Lakini hao hawakufanya yalio amrisha humo. Kwani wao walishika starehe ya dunia badala ya Neno la Haki. Wakijiambia nafsi zao: Mwenyezi Mungu atatusamehe kwa tunayo yatenda! Wakitaraji maghfira, na ilhali kuwa yakiwajia kama yale waliyo yashika watayashika vile vile. Basi wao wamekuwa wameshikilia kuendelea na madhambi pamoja na kutaka kwao msamaha. Tena basi Mwenyezi Mungu anawatahayarisha kwa vile kutaka maghfira na huku wanaendelea na yao, akasema: Sisi tulichukua kwao ahadi katika Taurati - nao wameyasoma yaliomo humo - kuwa waseme kweli; nao wakasema uwongo! Na hakika neema za nyumba ya Akhera za wanao jikinga na maasi ni bora kuliko starehe za duniani! Basi je, mtaendelea na uasi wenu, wala hayaingii akilini mwenu kuwa neema hizo ni bora kwenu? Na mnakhiari badala yake hizo starehe za dunia?

170 Na wanao ikamata baraabara Taurati, na wakashika Sala zilizo faridhiwa kwao, hakika Sisi hatutaupoteza ujira wao kwa sababu ya kutengeneza kwao na kutenda kwao mema.

171 Mwenyezi Mungu amejiibu kauli ya Mayahudi walipo sema kwamba Wana wa Israili hawakupata kwenda kinyume na Haki. Alisema: Ewe Nabii! Wakumbushe pale tulipo unyanyua mlima juu ya Wana wa Israili ukawa kama kiwingu, na wakafazaika kwa kuwa walidhani utawaangukia. Nasi tukawaambia wakati ule ulipo nyanyuliwa na wao wamo katika khofu: Yashikeni ya uwongofu tuliyo kupeni katika Taurati kwa nguvu na kuazimia ut'iifu. Na kumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kuzingatia na zitengene nafsi zenu kwa kuchamngu.

172. Na pale Mola wako Mlezi alipo waleta katika wanaadamu kutoka migongoni mwao kizazi chao, na akawashuhudisha juu ya nafsi zao, akawaambia: Je, Mimi si Mola Mlezi wenu? Wakasema: Kwani! Tumeshuhudia. Msije mkasema Siku ya Kiyama sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo.¹⁷²

173. Au mkasema: Hakika baba zetu ndio walio shirikisha kabla yetu, na sisi ni dhuriya zao tu baada yao. Basi utatungamiza kwa sababu ya waliyo yafanya wapotovu?¹⁷³

174. Ndio kama hivyo tunavyo zipambanua Ishara, kwa kutaraji kuwa watarejea.¹⁷⁴

175. Na wasomee khabari za yule ambaye tulimpa Ishara zetu, naye akajivua nazo. Na Shet'ani akamuandama, akawa miongoni walio potea.¹⁷⁵

176. Na tungelitaka tungeli mtukuza kwa hizo Ishara, lakini yeye aliushikilia ulimwengu na akafuata pumbao lake. Basi mfano wake ni mfano wa mbwa. Ukimhujumu hupumua na kutoa ulimi na ukimwacha pia hupumua na kutoa ulimi. Huo ni mfano wa kaumu wanao zikanusha Ishara zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari.¹⁷⁶

177. Huu ni mfano muovu kabisa wa watu wanao kanusha Ishara zetu na wakajidhulumu nafsi zao.¹⁷⁷

178. Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemhidi basi huyo amehidika; na alio waacha kupotea basi hao ndio walio khasirika.¹⁷⁸

172 Hapa Mwenyezi Mungu amebainisha hidaya ya wanaadamu kwa kusimamisha dalili katika viumbe, baada ya kwisha bainisha kwa njia za Mitume na Vitabu. Alisema: Ewe Nabii! Waambie watu pale Mola wako Mlezi alipo watoa kutoka migongo ya wanaadamu na watoto wao na wanao zaliwa karne baada ya karne, kisha akwasimamishia dalili za Ungu wake, na akawapa akili na nadhari ya kuwawezesha kuzijua, na kwa hizo akili na nadhari waweze kutambua Tawhidi na Rubuubiya, yaani kuwa Mwenyezi Mungu ni Mmoja Pekee na ni Mola Mlezi wa viumbe vyote, hata wakawa hao wanaadamu kama walio ulizwa: Je, Mimi siye Mola wenu Mlezi? Nao wakajibu: Kwani, Wewe ndiye Mola Mlezi wetu. Tunajishuhudia hayo juu ya nafsi zetu...Haya ni kwa kuwa kumkini kwao kupata kujua hizo hoja na dalili, na kutamakani kwao katika hayo imekuwa kama kwamba ni kukiri na kuungama. Na Sisi tumefanya haya ili msije kusema Siku ya Kiyama: Hakika sisi tulikuwa tumeghafilika na hiyo Tawhidi, na tulikuwa hatuijui. (*Tazama Maelezo 7:172*)

173 Au mtasema: Walishiriki baba zetu kabla yetu, na sisi ni dhuriya zao tumewafuata tu. Basi ewe Mola Mlezi wetu! Unatushika utuhiliki kwa walio yafanya wapotovu miongoni mwa baba zetu, kwa kujenga misingi ya ushirikina tulio endelea nao? Basi hamna hoja.

174 Kwa mfano wa maelezo wazi yenye hikima tunawabainisha wanaadamu dalili za kuwepo Mwenyezi Mungu, ili warejee waache ukhalifu wao na kuwafuata wapotovu.

175 Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa wanao kadhibisha kwa Aya zake alizomteremshia Mtume wake. Akasema: Ewe Nabii! Wasomee kaumu yako khabari za mtu mmoja katika Wana wa Israili. Tulimpa ilimu ya kuzijua Ishara tulizo wateremshia Mitume wetu. Yeye huyo akazipuuza, wala asizishughulikia. Basi Shetani akamfuata kwa khatua zake, na akamtawala kwa upotovu wake, akawa katika kundi la walio potea.

176 Na lau tungeli taka kumnyanyua afike daraja za watu wema, tungeli mnyanyua kwa kumwezesha kuyatenda maamrishi ya hizo Aya.. Lakini yeye alishikamana na dunia, na hakuweza kunyanyuka kwendea uwingu wa uwongo. Akafuata matamano yake. Akawa hali yake daima yumo katika dhiki, na kushughulika kwake ni kwa dunia, na tafakuri zake duniani ni kutaka kuipata hiyo dunia basi. Hali yake ni kama hali ya mbwa anapo kuwa katika hali ova kabisa, anavyo kuwa daima anapumua na kutoa limi lake nje, ukimkemea au ukimwacha. Hudorora ulimi wake kwa kuvuta pumzi kwa shida! Kadhaalika mwenye kuipenda dunia hudumu daima katika kuwania starehe zake na matamano yake! Hakika hizo ndizo sifa zinazo mueleza huyo mwenye kuziacha Aya zetu, na ndio sifa ya wote wanao zikadhibisha Aya zetu zilizo teremka. Basi wasimulie kisa chake hichi, huenda wakafikiri na wakaamini.

177 Ni mbaya kweli hali ya hao wanao zipinga Ishara zetu, na kwa huku kukengeuka kwao na kuacha Haki hakumdhulumu mtu ila nafsi zao tu.

178 Na yule ambaye Mwenyezi Mungu amemwezesha kufuata njia ya haki huyo basi ndie aliye ongoka

179. Na tumeiambia Jahannamu majini wengi na watu. Wana nyoyo, lakini hawafahamu kwazo. Na wana macho, lakini hawaoni kwayo. Na wana masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama nyama howa, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walio ghafilika.¹⁷⁹

180. Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo. Na waacheni wale wanao haribu utakatifu wa majina yake. Hao watakuja lipwa waliyo kuwa wakiyatenda.¹⁸⁰

181. Na katika tulio waumba wako watu wanao ongoza kwa Haki, na kwayo wanafanya uadilifu.¹⁸¹

182. Na wale walio kadhibisha Ishara zetu, tutawapururia pole pole kwa namna ambayo wenyewe hawajui.¹⁸²

183. Nami nitawapa muda. Hakika mpango wangu ni madhubuti.¹⁸³

184. Je, hawafikiri? Huyu mwenzao hana wazimu. Hakuwa yeye ila ni mwonyaji aliye dhaahiri.¹⁸⁴

185. Je, hawatazami ufalme wa mbingu na ardhi, na vitu alivyo viumba Mwenyezi Mungu, na pengine ajali yao imekwisha karibia? Basi maneno gani baada ya haya watayaamini?¹⁸⁵

186. Aliye mwacha Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumwongoa. Atawaacha hao wakitangatanga katika upotofu wao.¹⁸⁶

187. Wanakuuliza hiyo Saa (ya mwisho) itakuwa lini? Sema: Kuijua kwake kuko kwa

kweli, mwenye kupata furaha ya kote kuwili duniani na Akhera. Na mwenye kukosa uwezesho huo kwa sababu ya kumilikiwa na pumbao lake basi watu hao ndio walio khasiri.

179 Na tumewaambia wengi katika majini na watu marejeo yao ni Motoni Siku ya Kiyama. Kwani hao wana nyoyo zisio funguka ikaingia Haki ndani yake. Wana macho yasiyo angalia dalili za kudra. Wana masikio yasiyo sikia Aya na mawaidha kwa sikio la kuzingatia na kuwaidhika! Hao ni kama wanyama kwa kutonafika kwa neema ya akili za kuzingatia walizo neemeshwa na Mwenyezi Mungu. Bali hao ni wapotovu zaidi kuliko wanyama, kwani wanyama hutaka cha kuwafaa na hukimbia cha kuwadhuru. Lakini hawa watu hata hawatambui hayo. Hao ndio walio fikia ukomo wa kughafilika.

180 Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye Majina yenye kuonyesha sifa za ukamilifu. Basi mtumilieni hayo mnapo muomba, au mnapo mwita au kumtaja. Na waepukeni hao wanao mili katika hayo yasiyo elekeana na dhati ya utukufu wake. Hao watakuja lipwa malipo ya vitendo vyao.

181 Na katika tulio wajaalia waingie Peponi wapo wanao waita wengineo kwenye Haki kwa kuipenda Haki, na kwa Haki tu wanafanya uadilifu katika hukumu zao.

182 Na wale walio zikanusha Ishara (Aya) zetu zililo teremshwa tutawapururia pole pole, na tutawawacha mpaka wafike ukomo watapo fika. Na hayo ni kwa kuwapururia neema juu yao, juu ya kushughulika kwao katika maasi, mpaka maangamizo yawazukie nao wameghafilika wakitaladhadhi na starehe zao.

183 Nitawakunjulia maisha, bila ya kuyapuza maovu yao. Na mipango yangu niliyo wapangia ni ya nguvu na mikali juu yao, inalingana na madhambi yao yaliyo zidi kwa kupita kiasi.

184 Wao wameanza kwa kukadhibisha, wala hawakuzingatia yale anayo waitia kwayo Mtume, na hoja anazo zitoa. Bali wakamsingizia kuwa ni mwendaazimu, na hali hana wazimu chochote. Yeye huyu ni mwenye kuwaonya wasifikwiwe na adhabu ya ushirikina wao. Na onyo lake liwazi, la dhaahiri.

185 Wamemwambia Muhammad mwongo kwa Tawhidi anayo waitia, wala hawakutazama kwa kuzingatia na kutafuta dalili za ufalme mtukufu wa Mwenyezi Mungu ulioko katika mbingu na ardhi na viliomo ndani yao, zinazo onyesha ukamilifu wa uwezo wa huyu Mwenye kuunda, na zinazo onyesha Umoja wake wa pekee. Wala hawakufikiri kuwa ajali yao imekwisha karibia, au huenda ikawa imekaribia, wapate kufanya haraka kutupia nadhari na kuitafuta Haki kabla ya kuzuka ajali. Ikiwa basi watu hawa hawaamini maneno ya Qur'ani watakuja amini maneno gani baada yake.

186 Aliye andikiwa na Mwenyezi Mungu kupotea kwa uwovu wa uchaguzi wake mwenyewe, basi hapana mtu wa kumhidi. Na Yeye Subhana, Aliye takasika, anawaacha watu kama hao wakihangaika wala hawaitambui njia.

Mola Mlezi wangu. Haidhihirishi hiyo kwa wakati wake ila Yeye. Ni nzito katika mbingu na ardhi. Haikujii ni ila kwa ghafla tu. Wanakuuliza kama kwamba wewe una pupa ya kuijua. Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Lakini aghlabu ya watu hawajui.¹⁸⁷

188. Sema: Siimiliki nafsi yangu manufaa wala madhara, ila apendavyo Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ninge jizidishia mema mengi, wala ovu lisinge nigusa. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini.¹⁸⁸

189. Yeye ndiye aliye kuumbeni katika nafsi moja; na katika hiyo akamfanya mwenzi wake, ili akae naye kwa utulivu. Na anapo muingilia hubeba mzigo mwepesi, akitembea nao. Anapo kuwa mja mzito, wote wawili humwomba Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wao: Kama ukitupa mwana mwema tutakuwa katika wanao shukuru.¹⁸⁹

190. Basi anapo wapa mwana mwema, wanamfanyia washirikina Mwenyezi Mungu katika kile alichu wapa. Mwenyezi Mungu ametukuka na huko kushirikisha kwao.¹⁹⁰

191. Ati wanawafanya viumbe kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu, nao hawaumbi, bali wao ndio wanaumbwa?¹⁹¹

192. Wala hawana uwezo wa kuwanusuru wala wenyewe hawajinusuru.¹⁹²

193. Na mkiwaita kwenye uwongofu, hawakufuateni. Ni mamoja kwenu ikiwa mtawaita au mkinyamaza.¹⁹³

194. Hakika hao mnao waomba asiye kuwa Mwenyezi Mungu ni waja mfano wenu

187 Ewe Muhammad! Mayahudi wanakuuliza khabari ya Saa itakayo malizikia dunia. Itakuwa wakati gani, kujulikana khasa? Waambie: Ujuzi wa wakati wake uko kwa Mwenyewe Mola wangu Mlezi peke yake. Haujui wakati wake mtu yeyote isipo kuwa Yeye. Itapo tokea kitisho chake kitakuwa kikuu kwa walioko mbinguni na ardhi! Wao wanakuuliza suala hili kama kwamba wewe una pupa ya kuijua! Basi wakaririe jawabu, na uwambie kwa kutia mkazo: Hakika kuijua hiyo Saa kuko kwa Mwenyezi Mungu, lakini aghlabu ya watu hawatambui hakika ya wasiyo yaona au wanayo yaona!

188 Waambie: Mimi siimiliki nafsi yangu kujiletea nafuu, wala kujikinga na madhara, ila Mwenyezi Mungu akipenda hayo. Hapo ndio hunipa mamlaka. Na lau kuwa mimi najua yale yaliyo fichikana kwangu, kama mnavyo dhani, basi ningeli kithirisha kila kheri, kwa kuwa ninajua sababu zake. Na ninge ilinda nafsi yangu na kila ovu, kwa kuyaepuka yanayo leta madhara. Mimi si chochote ila ni mwonyaji wa adhabu, na mbashiri wa thawabu, kwa kaumu wanayo iamini Haki na wanait'ii.

189 Yeye ndiye Allah, Mwenyezi Mungu, aliye kuumbeni hapo mwanzo kwa nafsi moja. Na akajaalia katika nafsi ile ile mwenzie, na vizazi vyao vikaendelea kuwepo. Nanyi mlikuwa mume na mke. Basi alipo muingilia akachukua mzigo mwepesi, nayo ndio mimba changa, inapo kuwa kama pande la damu na pande la nyama. Mimba ikiwa nzito katika tumbo lake huyo mke, mume na mke humwomba Mola wao Mlezi wakisema: Wallahi, ukitupa mwana mzima asiye na ila katika umbo lake, tutakushukuru kwa neema yako.

190 Akisha wapa wakitakacho, huwafanya masanamu ndio washirika wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika ile zawadi yake ya ukarimu, kwa kuyatambikia kama kwamba ndio wanayashukuru. Na Mwenyezi Mungu pekee ndiye anaye stahiki kushukuriwa. Yeye ametukuka, hawezi kuwa kama hiyo miungu yao ya kishirikina.

191 Jee, inawafalia kumshirikisha Mwenyezi Mungu na masanamu yasio weza kuumba kitu, bali hayo yameumbwa na Mwenyezi Mungu?

192 Wala hayawezi kuwasaidia hao wanayo yaabudu, wala hayajisaidii wenyewe akitokea mtu kuyashambulia.

193 Na nyinyi mnao yaabudu masanamu! Mkiyaomba hayo masanamu yakuongozeni mpate mnacho kipenda hayakuitikieni hayo myatakayo! Ni sawa sawa kwenu kuwa hapana faida ya kuwaomba au mkinyamaza. Hali yao haibadiliki vyo vyote vile.

nyinyi. Hebu waombeni, nao wakuitikieni, kama mnasema kweli.¹⁹⁴

195. Je, wao wanayo miguu ya kwendea? Au wanayo mikono ya kutetea? Au wanayo macho ya kuonea? Au wanayo masikio ya kusikizia? Sema: Iiteni hio miungu yenu ya ushirikina. Kisha nifanyieni mimi vitimbi, wala msinipe muhula.¹⁹⁵

196. Hakika Mlinzi wangu ni Mwenyezi Mungu aliye teremsha Kitabu. Naye ndiye awalindae walio wema.¹⁹⁶

197. Na hao mnao waomba asiye kuwa Mwenyezi hawawezi kukunusuruni, wala hawajinusuru wenyewe.¹⁹⁷

198. Na mkiwaita kwenye uwongofu hawasikii. Na unawaona wanakutazama, nao hawaoni.¹⁹⁸

199. Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili.¹⁹⁹

200. Na uchochezi wa Shet'ani ukikuchochea basi omba ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Msikizi, Mjuzi.²⁰⁰

201. Hakika wale wamchao Mungu, zinapo wagusa pepesi za Shet'ani, mara huzindikana na hapo huwa wenye kuiona haki.²⁰¹

202. Na ndugu zao wanawavutia kwenye upotofu, kisha wao hawaachi.²⁰²

203. Na usipo waletea Ishara waitakayo husema: Kwa nini hukuibuni? Sema: mimi ninafuata yanayo funuliwa kwangu kutokana na Mola Mlezi wangu. Hii (Qur'ani) ni hoja zinazo toka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu na rehema kwa watu wanao amini.²⁰³

194 Hakika hao mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, na mkataraji nafuu kwao, wao wenyewe wanamnyenyekea Mwenyezi Mungu kwa hukumu ya maumbile yao. Kwani Yeye Mwenyezi Mungu amewafanya wafuate amri yake mfano wenu nyinyi. Kama nyinyi mnasema kweli katika madai yenu kuwa hao wanaweza lolote, basi watakeni, na wao wakutimilizieni.

195 Bali haya masanamu ni duni kuliko nyinyi kwa kuumbwa na kuwa! Kwani wao wana miguu ya kuendea? Au wana mikono ya kuingia madhara yasikupateni au yasiwapate wenyewe? Au wana macho ya kuonea? Au masikio ya kusikia hayo mnayo yataka wakakupeni? Hawana chochote katika hayo! Vipi basi mnawashirikisha hao na Mwenyezi Mungu? Na ikiwa nyinyi mnadhani kuwa hio miungu ya uwongo inaweza kunidhuru mimi au mtu yeyote, basi iiteni, na mfanye njama zenu pamoja nao kama mtakavyo, bila ya kunipa muhula wala kungoja. Hao hakika hawawezi kitu! Basi msiningojee, na wala mimi siwabali.

196 Hakika msaidizi wangu wa kuninusuru nanyi ni Yeye Mwenyezi Mungu. Ulinzi wangu uko kwake. Naye ndiye aliye niteremshia Qur'ani. Na Yeye peke yake ndiye anaye wanusuru waja wake walio wema.

197 Na hayo masanamu mnayo taka kwao msaada, badala ya Mwenyezi Mungu, hayawezi kukusaidieni nyinyi, wala kujisaidia wenyewe.

198 Na ukiwataka uwongofu katika yaliyo na kheri nanyi hawalisikii ombi lenu, licha ya kukuongozeni! Unawaona wanavyo kukabili kama kwamba wanakutazama, na kumbe wao kwa hakika hawaoni kitu!

199 Ewe Nabii! Waachilie mbali hao majaahili, na endelea katika njia ya Da'wa (Wito). Na wachukulie watu kwa lilio wepesi kwao. Na waamrishe kila jambo linalo pendeza na kuingia akilini.

200 Na Shetani akikuchochea kwa wasiwasi ili apate kukuachisha ulio amrisha, kama vile kukasirika kwa kukushikilia kwao mambo ya shari, basi omba ulinzi wa Mwenyezi Mungu akuepushe naye huyo Shetani. Kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na kujua kila linalo tokea.

201 Hakika wale wamchao Mola wao Mlezi, na wakaweka baina yao na maasi kinga cha kuzuia uchochezi wa Shetani unao wapitia kuwaachisha yaliyo waajibu wao, hukumbuka uadui wa Shetani na vitimbi vyake. Kwa hivyo hao wanaiona Haki, basi ndio wanarejea.

202 Na ndugu zao mashetani, nao ni hao makafiri, mashetani huwazidisha upotovu kwa kuwajaza wasiwasi. Tena hawa makafiri hawaachi upotovu wao wakazingatia.

203 Na usipo waletea makafiri Ishara wanayo itaka kwa inadi na ukafiri, husema: Kwa nini hukuitaka? (au hukuizua? Makusudio yao ni kuwa Mtume s.a.w. akizibuni Aya zote.) Waambie: Mimi sifuiti ila Qur'ani ninayo funuliwa kwa wahyi kutoka kwa Mola wangu Mlezi. Na waambie: Hii Qur'ani ni hoja zinazo toka

204. Na isomwapo Qur'ani isikilizeni na mnyamaze ili mpate kurehemewa.²⁰⁴

205. Na mkumbuke Mola Mlezi wako nafsini kwako kwa unyenyekevu na khofu, na bila ya kupiga kelele kwa kauli, asubuhi na jioni. Wala usiwe miongoni wa walio ghafilika.²⁰⁵

206. Hakika wale walioko kwa Mola wako Mlezi hawajivuni wakaacha kumuabdu, na wanamtakasa na wanamsujudia.²⁰⁶

kwa Mola Mlezi wenu kukuonyesheni njia za Haki. Nayo ina uwongofu, na rehema, kwa Waumini, kwa sababu wao wanaifuata kwa vitendo.

204 Enyi Waumini! Mkisomewa Qur'ani isikilizeni kwa masikio yenu, mpate kuzingatia mawaidha yake, na msikilize vizuri mpate kuipata rehema.

205 Na mtaje Mola wako Mlezi ndani ya nafsi yako, upate kuhisi kuwa upo karibu na Mwenyezi Mungu, kwa kumnyenyekea na kumkhofu, bila ya kupiga makelele, bali juu kidogo kuliko kwa siri, na chini ya kudhihirisha kwa maneno. Na umtaje na umkumbuke asubuhi na jioni, ili uanzie mchana wako kwa kumkumbuka Mola wako Mlezi, na ukhitimishie kwayo vile vile. Na wakati wako wote usighafilike na kumtaja na kumkumbuka Mwenyezi Mungu.

206 Hao walio karibu na Mola wako Mlezi kwa utukufu na takrimu hawatakabari wakaacha kumuabudu. Na wanamtakasa Mwenyezi Mungu na kila lisio faa kwake. Na wanamnyenyekea Yeye.

Sura 8 - Al-Anfaal

Utangulizi

Surat Al Anfaal hii imeteremka Madina. Aya zake ni 75. Mwenyezi Mungu aliye takasika na kutukuka, amebainisha katika Sura hii baadhi ya hukumu za vita, na mambo yanayo pelekea vita, na sababu za ushindi, na makamo ya nguvu za moyo zinazo pelekea kushinda, na hukumu za ngawira za vita, na wakati gani kuchukua mateka. Na Mwenyezi Mungu kwa hikima yake amekusanya humu hukumu za kisharia. Sura hii inaeleza kisa cha Vita vya Badri, na baadhi ya yaliyo kuwa kabla yake, na kuashiria sababu zilizo sabibisha hivyo vita, nazo ni kutoka makafiri washirikina Makka kumwendea Nabii s.a.w.. Na humu Mwenyezi Mungu anataja kujitayarisha kwa vita, na kupasa kuelekea salama na amani ikiwa maadui wanaelekea kutaka salama. Na Sura hii tukufu inamalizikia kubainisha urafiki wa Waumini, wao kwa wao; na kuwawajibikia Waumini kuihama nchi inayo waonea na kuwafanya wanyonge, ili wende kuwaunga mkono Waumini wenzao katika juhudi ya kutukuza Uislamu na Waislamu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU.

1. Wanakuuliza juu ya Ngawira. Sema: Ngawira ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume. Basi mcheni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu, na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ikiwa nyinyi ni Waumini.¹
2. Hakika Waumini ni wale ambao anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanapo somewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi.²
3. Hao ambao wanashika Sala na wanatoa katika yale tunayo waruzuku.³

1 Nabii Muhammad (s.a.w.) katolewa Makka na kalazimishwa kuihama kwa sababu ya vitimbi vya mapagani, washirikina, na kwa kuazimia kwao kumuwa, ili Waislamu wapate kuwa na dola yao. Naye akenda kukaa Madina kwenye amani na manusura. Huko ikawa hapana budi ila kuwania kujilinda na uvamizi wa maadui, wasije wenye Imani wakapata mateso. Vikatokea hivyo Vita vya Badri. Waumini wakapata ushindi ulio wazi na ngawira nyingi waliziteka. Ikatokea khitilafu kidogo na suala katika shauri la ugawaji wa hizo ngawira. Ndio hivyo Mwenyezi Mungu anasema: Wanakuuliza khabari ya ngawira, zende wapi? Apewe nani? Ni za nani? Zigawanywe vipi? Ewe Nabii! Waambie: Hizo ngawira ni za Mwenyezi Mungu kwanza. Na Mtume, kwa amri ya Mola wake Mlezi, ndiye mwenye madaraka ya kuzigawa. Basi wacheni kukhitalifiana kwa ajili ya hayo. Na uwe mtindo wenu ni kumkhofu Mwenyezi Mungu na kumt'ii. Na tengenezeni yaliyo baina yenu, na mfanye mapenzi na uadilifu ndio makhusiano baina yenu. Kwani hakika hizi ndizo sifa za watu wa Imani.

2 Ama hakika Waumini wa haki na kweli daima wanakuwa na khofu na ut'iifu kwa Mwenyezi Mungu. Akitajwa Allah *Subhanahu*, Mwenyezi Mungu Aliye takasika, nyoyo zao hufazaika, na zikajaa khofu. Kwa hivyo kila wakisomewa Aya za Qur'ani Imani yao inazidi kuwa imara, na wao huzidi unyenyekevu na ujuzi, na wala hawamtegemei yeyote ila Mwenyezi Mungu aliye waumba, na ndiye anaye walinda na kuwaendeleza.

3 Na hao Waumini walio wa kweli katika Imani, wanashika Sala kwa kutimiza nguzo zake, na kukamilisha unyenyekevu na ut'iifu, ili wawe daima katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu, na wanatoa katika mali aliyo waruzuku Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la*, kwa ajili ya Jihadi, na mambo yote ya kheri, na

4. Hao kweli ndio Waumini. Wao wana vyeo, na maghfira, na riziki bora, kwa Mola wao Mlezi.⁴
5. Kama Mola wako Mlezi alivyo kutoa nyumbani kwako kwa Haki, na hakika kundi moja la Waumini linachukia.⁵
6. Wanajadiliana nawe kwa jambo la Haki baada ya kwisha bainika, kama kwamba wanasukumwa kwenye mauti nao wanaona.⁶
7. Na Mwenyezi Mungu alipo kuahidini kuwa moja katika makundi mawili ni lenu. Nanyi mkapenda lisilo na nguvu ndio liwe lenu; na Mwenyezi Mungu anapenda ahakikishe Haki kwa maneno yake, na aikate mizizi ya makafiri.⁷
8. Ili ahakikishe Haki na auvunje upotovu na wangachukia wakosefu.⁸
9. Mlipo kuwa mkimuomba msaada Mola wenu Mlezi, naye akakujibuni kuwa: Kwa yakini Mimi nitakusaidieni kwa Malaika elfu wanao fuatana mfululizo.⁹
10. Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara na ili nyoyo zenu zituwe. Na haupatikani ushindi ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, na Mwenye hikima.¹⁰
11. Alipo kufunikeneni kwa usingizi uwe ni uaminisho kutoka kwake, na akakuteremshieni maji kutoka mbinguni ili kukusafisheni kwayo na kukuondoleeni uchafu wa Shet'ani,

kuwasaidia wanyonge.

4 Hakika hawa wanao sifika kwa sifa hizi ndio khasa wanao sifika kwa Imani kwa haki na kweli. Na malipo yao ni kupata vyeo vya ngazi ya juu kwa Mwenyezi Mungu. Yeye Allah *Subhanahu* ndiye ataye wapa radhi zake, na maghafira wanapo teleza, na duniani atawapa riziki njema, na Akhera neema ya daima.

5 Ushindi, bila ya shaka, upo mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Na funguo za mambo yote ziko kwake. Na hali ya Waumini katika kukhitalifiana kwao katika mambo ya ngawira ni kama hali yao pale alipo kuamrisha Mwenyezi Mungu utoke ukapigane na washirikina katika Badri, nayo ni Haki iliyo thibiti. Kwani miongoni mwa Waumini kulikuwapo na kikundi kilicho chukia vita kweli kweli.

6 Wanajadiliana nawe hao wa kikundi hicho, na wanajaribu kutilia nguvu kauli yao katika jambo la haki, nalo ni kutoka kwa ajili ya Jihadi. Na kumbe wao walikuwa na wenzao walio toka kwenda kupokonya mali ya Makureshi yaliyo kuwa yanakwenda Sham, na wasiyapate. Kikundi hichi kikakhiari kurejea baada ya kuona wamenusurika, kwa kujuvywa na Mtume, na kwamba makafiri wanawaogopa, na kwa kuwa hadi wakivichukia vita, na kuwa hawajui litalo wapata. Na walipo kuwa wakiviendea vita walikuwa kama wanao sukumba kwenda kufa, na wao wanaona kitacho wauwa, na yanawapata mateso yake.

7 Enyi Waumini! Kumbukeni ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwenu kwamba atakupeni ushindi juu ya moja katika makundi mawili, hilo lenye silaha na nguvu. Na hali nyinyi mnapendelea kupambana na hilo kundi jengine lenye mali na watu tu. Na hilo ni msafara wa Abu Sufyan. Nanyi mkakhiari mali yasiyo kuwa na wapiganaji. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka kuithibitisha Haki kwa mapendo yake na uwezo wake na kwa maneno yake yaliyo kwisha tangazwa, na ili aung'oe kabisa ukafiri katika Bara Arabu kwa ushindi wa Waumini. (*Tazama Maelezo 8:7*)

8 Ili athibitisha Haki, na auondoe upotovu, hata wakichukia makafiri ambao wamedhulumu Haki ya Mwenyezi Mungu na Haki ya Waumini na Haki ya nafsi zao wenyewe.

9 Na enyi Waumini! Kumbukeni nanyi mnagawana ngawira na mnakhitalifiana, mlipo omba uwokovu na msaada, na mkaandikiwa kuwa hapana la kukuepusheni na vita. Mwenyezi Mungu alikuitikieni maombi yenu, akakuungeni mkono kwa kukuleteeni (Malaika) Roho zilizo safi nyingi zinazo fika elfu zinazo fuatana, zikija moja baada ya moja. (*Tazama Maelezo 8:9*)

10 Wala Mwenyezi Mungu Mtukufu hakujaalia huko kukuungeni mkono kwa (Malaika) hizo Roho safi ila ni kuwa ni kukupeni khabari njema, kama bishara kwenu kuwa mtashinda, mpate kutua nyoyo na msonge mbele. Na Mwenyezi Mungu anakusaidieni, na wala ushindi hauji ila kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye kushinda, ambaye anaye panga mambo kwa pahala pake kwa mujibu wa ujuzi wake usio pitikiwa na chochote.

na kuzipa nguvu nyoyo zenu, na kuitia imara miguu yenu.¹¹

12. Mola wako Mlezi alipo wafunulia Malaika: Hakika Mimi ni pamoja nanyi, basi watieni nguvu walio amini. Nitatia woga katika nyoyo za walio kufuru. Basi wapigeni juu ya shingo na wapigeni kwenye kila ncha za vidole.¹²

13. Hayo ni kwa sababu wamemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.¹³

14. Ndio hivyo! Basi ionjeni! Na bila ya shaka makafiri wana adhabu ya Moto.¹⁴

15. Enyi Mlio amini! Mkikutana na walio kufuru vitani msiwageuzie mgongo.¹⁵

16. Na atakaye wageuzia mgongo wake siku hiyo - isipo kuwa kwa mbinu za vita au kuungana na kikosi - basi atakuwa amestahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na pahala pake ni Jahannamu, na huo ni mwisho muovu.¹⁶

17. Hamkuwauwa nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye wauwa. Na wewe hukutupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye tupa, ili awajaribu Waumini majaribio mema yatokayo kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Msikizi na Mjuzi.¹⁷

18. Ndio hivyo! Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kudhoofisha vitimbi vya makafiri.¹⁸

11 Enyi Waumini! Kumbukeni wakati mlipo ingiwa khofu kwa upungufu wa maji, na kuwaogopa maadui. Mwenyezi Mungu alikupeni utulivu, kwa kukuleteeni usingizi, mkalala mkatua. Akakuteremshieni maji kutoka mbinguni mkajisafishia, na mkaoundoa wasiwasi wa Shetani, na nyoyo zenu zikawa imara kwa msaada wa Rahmani na pia ardhii ikashikamana kwa hayo maji, na miguu yenu ikaweza kukanyaga bila ya kudidimia katika mchanga. (*Tazama Maelezo 8:11*)

12 Enyi Waumini! Kumbukeni pale Mwenyezi Mungu alipo wafunulia wale wenye Roho zililo t'ahirika, yaani Malaika, watie ndani ya nyoyo zenu kuwa Mimi ni pamoja nanyi, nakuungeni mkono, na ninakusaidieni, kwa kuwaambia: Zitieni nguvu nyoyo za walio amini, wait'ii Haki na wapigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Na Mimi nitaifanya khofu izitawale nyoyo za washirikina, nao watakuogopeni. Nanyi enyi Waumini! Wapigeni vichwani mwao vilio juu ya shingo zao, na kateni vidole vyao vinavyo kamata panga.

13 Ukawa ushindi na kuungwa mkono nyinyi, na kwao ni kitisho na fazaa, kwani wao walikuwa upande mmoja, na Mwenyezi Mungu na Mtume wake walikuwa upande mwengine, kwa kuwa wao walimpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Basi ndio Mwenyezi Mungu anawateremshia adhabu chungu. Na adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali.

14 Enyi Waumini! Hivyo ndio vita, basi vionjeni, na muwe na yakini kuwa mpatata nusura na kuungwa mkono. Na wanao pinga Ishara za Mwenyezi Mungu watapata adhabu nyengine Siku ya Kiyama, nayo ni adhabu ya Moto.

15 Enyi mlio isadiki Haki na mkait'ii! Mkikutana na wale walio kufuru katika uwanja wa vita nao wanakujieni kwa wingi wao, msiwakimbie mkazipa mgongo panga zao.

16 Na asiye wakaabili uso kwa uso, basi Mwenyezi Mungu amekasirika naye, na marejeo yake ni Motoni. Na huo ndio mwisho muovu kweli. Na mwenye kuacha kuwakaabili kwa kuwa ni hila na mbinu za vita, au kaacha kikosi kwenda jiunga na kikosi kingine cha Waumini apate kuwa na nguvu zaidi za mpambano, huyo hana dhambi.

17 Na nyinyi Waumini, pale mnapo washinda, na mkawauwa mlio wauwa katika wao, basi hakika si nyinyi mlio wauwa kwa nguvu zenu, lakini ni Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliye kupeni ushindi na kuweza kuwauwa, kwa msaada wake kwenu na kutia khofu katika nyoyo zao. Na wewe Mtume, pale ulipo warushia mchanga na kokoto nyusoni mwao kuwafazaisha, si wewe ulio rucha, lakini ni Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliye rucha, na wao wakafazaika. Na hayo Mwenyezi Mungu ameyafanya kuwaneemesha Waumini kwa neema njema. Katika hayo pana majaribio ya nguvu kwao, ili ionekane ikhlasi yao, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua mambo yao, Mwenye kusikia maneno yao, na Mwenye kujua mambo ya maadui zao na kauli zao pia.

18 Huo ndio ushindi mkubwa, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mwenye kudhoofisha kila hila za

19. Kama mnataka hukumu basi hukumu imekwisha kujieni. Na mkiacha itakuwa ndio kheri kwenu. Na mkirejea Sisi pia tutarejea. Na jeshi lenu halitakufaeni kitu, japo likiwa kubwa. Kwani hakika Mwenyezi yu pamoja na Waumini.¹⁹

20. Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msijiepushe naye, nanyi mnasikia.²⁰

21. Wala msiwe kama wale wanao sema: Tumesikia, na kumbe hawasikii.²¹

22. Hakika vinyama viovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni vile viziwi na bubu visio tumia akili zao.²²

23. Na Mwenyezi Mungu angeli jua wema wowote kwao ange wasikilizisha, na lau ange wasikilizisha wangeli geuka wakapuza.²³

24. Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa.²⁴

25. Na jikingeni na Fitna ambayo haitowasibu walio dhulumu peke yao kati yenu. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.²⁵

26. Na kumbukeni mlipo kuwa wachache, mkionekana wanyonge katika nchi, mnaogopa watu wasikunyakueni, naye akakupeni pahala pazuri pa kukaa, na akakutieni nguvu kwa nusura yake, na akakupeni riziki nzuri ili mpate kushukuru.²⁶

makafiri.

19 Ikiwa nyinyi washirikina mlikuwa mkining'inia mapazia ya Al Kaaba na huku mnaomba yapambanuliwe baina yenu na Waumini ijuulikane haki ipo wapi, basi sasa imekwisha kujieni hukumu ya kupambanua, na ushindi si wenu, bali ni wa Waumini. Na nyinyi mkirejea tena kufanya uadui Nasi tutakushindeni tena. Wala kukusanyika kwenu kwa ajili ya madhambi hakutakufaeni kitu! Hata ikiwa idadi yenu kubwa vipi! Kwani hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao isaidiki Haki na wanaikubali.

20 Enyi mlio isadiki Haki, na mkaifuata! Hakika mmejua ushindi umepatikana kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na kumt'ii Mtume wake. Basi endeleeni kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume. Wala msiupuuze wito wa Mtume anao itia Haki, nanyi mnamsikia na mnafahamu ayasemayo.

21 Wala msiwe kama wanaafiki wanao sema: Tumeisikia Haki na tumefahamu. Lakini hawaiifuati wala hawaiamini. Basi wamekuwa kama wasio sikia.

22 Hao washirikina na wanaafiki ni kama wanyama waovu kabisa walio sibiwa na uziwi, kwa hivyo hawasikii; na wakasibiwa na ububu, kwa hivyo hawasemi. Basi wao ni viziwi kwa Haki, na hivyo hawasikii, wala hawaitamki na hawaelewi!!

23 Na Mwenyezi Mungu kwa ilimu yake ya tangu na tangu lau angeli ona ndani yao kuwa, katika hali yao hivi sasa, itakuja patikana kheri yoyote kwao hao kwa nafsi zao, na kwa watu, na kwa Haki, basi angeli wafanya wasikie kusikia kwa kuongoka hata Haki ikaingia akilini mwao. Na hata wangeli isikia na wakaifahamu Haki basi bado wasingeli ifuata. Na mapuza hayawaachi kwa kuzidiwa na pumbao.

24 Enyi mlio isadiki Haki na mkaifuata! Muitikieni Mwenyezi Mungu kwa kufikisha anayo kuamrishi. Na muitikieni Mtume katika vile anvayo fikisha anayo yaamrisha Mwenyezi Mungu, pale anapo kuiteni Mtume kufuata amri za Mwenyezi Mungu ambazo zitakuleteni uzima wa miili yenu, na roho zenu, na akili zenu, na nyoyo zenu. Na mjue kwa yakini kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenya kuangalia nyoyo zenu. Huzielekeza atakavyo. Basi Yeye huingilia baina yenu na nyoyo zenu zinapo ingiliwa na matamano, Yeye basi hukuokoeni nayo ikiwa nyinyi wenyewe mnajielekeza kwenye Njia iliyo nyooka. Na nyinyi nyote mtakusanywa kwake Siku ya Kiyama, na huko ndiko malipo yatakuwa.

25 Na jikingeni na Dhambi kubwa ya kufisidi jamii yenu, kama vile kuacha kwenda kwenye Jihadi, na kufarikiana mkagawana mapande mapande, na kama kuacha kuamrisha mema na kukataza maovu. Kwani Fitna hiyo, Dhambi hiyo, haiwapati wale walio dhulumu peke yao, bali inawapata wote. Na mjue kuwa bila ya shaka kuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali hapa duniani na Akhera pia.

26 Na hebu kumbukeni, enyi Waumini, katika hali ya kuwa mna nguvu, pale mlipo kuwa wachache na wanyonge. Maadui walikudhilini kwa unyonge wenu, nanyi mlshikwa na khofu wasije maadui zenu kukunyakueni. Basi tena mkahama kwa amri ya Mwenyezi Mungu, na makaazi yenu yakawa Yathrib

27. Enyi mlio amini! Msimfanyie khiana Mwenyezi Mungu na Mtume, wala msikhini amana zenu, nanyi mnajua.²⁷
28. Na jueni ya kwamba mali zenu na wana wenu ni Fitna (mtihani), na kwamba kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa.²⁸
29. Enyi mlio amini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atakupeni kipambanuo, na atakufutieni makosa, na atakusameheni, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa.²⁹
30. Na walipo kupangia mpango walio kufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango.³⁰
31. Na wanapo somewa Aya zetu, wao husema: Tumesikia. Na lau tungeli penda tunge sema kama haya. Haya si chochote ila hadithi za watu wa kale tu.³¹
32. Na walipo sema: Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako basi tunyeshee mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyo chungu.³²
33. Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaadhibu nawe umo pamoja nao, wala Mwenyezi Mungu si wa kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha.³³
34. Lakini wana jambo gani hata Mwenyezi Mungu asiwaadhibu, na hali ya kuwa wanawazuilia watu Msikiti Mtakatifu? Wala wao hawakuwa ndio walinzi wake, bali walinzi wake hawakuwa ila wacha-Mngu tu. Lakini wengi katika wao hawajui.³⁴

(Madina). Na mkapata manusura kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na tawfiki yake, na akakuruzukuni ngawira njema kutaraji mtashukuru kwa neema hii, na muendele katika Njia ya Jihadi kulinyanyua Neno la Haki.

27 Enyi mlio isadiki Haki mkaifuata! Haikufaliini kumkhini Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kufanya urafiki na maadui wa Haki, na kukhuni katika ngawira, au kwa kuacha kwenda kwenye Jihadi. Wala msikhuni amana mnazo pewa nanyi mnajua amri na makatazo yake.

28 Enyi Waumini, wenye kusadiki! Jueni kuwa fitna ya nafsi zenu inatokana na kupita mpaka katika mapenzi yenu kwa watoto wenu na mali yenu. Basi isiwe kupenda kwenu kuyapenda mali na wenenu yakazidi kuliko mapenzi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hayo yatakuharibieni mambo yenu. Na jueni kuwa malipo ya Mwenyezi Mungu yanakutosheni kuliko mali na watoto.

29 Enyi mlio isadiki Haki na mkaifuata! Mkizinyenyekea amri za Mwenyezi Mungu kwa siri na dhaahiri, Mwenyezi Mungu atakujaalieni katika nafsi zenu uwezo wa kupambanua baina ya Haki na upotovu, na atakutunukieni ushindi wa kutenga baina yenu na maadui zenu, na atakusitirieni maovu yenu yaondoke, naye akusameheni. Na Yeye *Subhanahu* daima ni Mwenye fadhila kubwa.

30 Na kumbuka ewe Nabii, neema za Mwenyezi Mungu zilio juu yako, pale washirikina walipo panga njama kukutia nguvuni - ama wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe mji! Hakika walikupangia mipango miovu! Na Mwenyezi Mungu Mtukufu alikupangia utokane na shari yao. Na mpango wa Mwenyezi Mungu ndio wa kheri, na una nguvu zaidi, na ndio wenye kushinda.

31 Na ewe Nabii! Kumbuka inda ya washirikina ulipo kuwa ukiwasomea Aya za Qur'ani Tukufu, nazo ni Ishara zetu. Ujahili wao na ghururi yao iliyo pita kiasi iliwapelekea kusema: Tungeli taka kusema kama isemavyo hii Qur'ani tungeli sema; kwani humu hamna chochote ila visa walivyo viandika watu wa kale!

32 Na kumbuka, ewe Nabii, vipi walivyo kuwa wanakupinga na kumpinga Mwenyezi Mungu hata kwa inda yao wakasema kumwambia Mwenyezi Mungu, Mola wao Mlezi: Ikiwa haya unayo kuja nayo ni mambo madhbuti, basi zijaalie mbingu zitunyeshee mawe, au tulettee adhabu yoyote iliyo kali yenye uchungu!

33 Si katika hikima ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwaadhibu katika dunia kwa adhabu kali na hali wewe upo miongoni mwao unaitia Haki, nawe unataraji asaa wataitikia. Wala si mtindo wa Mwenyezi Mungu kuwaadhibu wenye kuasi nao wangali wanamuomba maghfira na wamo kuyavua yale waliyo nayo.

34 Hakika hali yao iliyo sasa inaruhusu kuwaadhibu, kwani wanawazuia watu wasiutumie Msikiti ambao Mwenyezi Mungu ameutukua kwa kuharimisha vita karibu yake. Lakini Mwenyezi Mungu

- 35.** Na haikuwa ibada yao kwenye hiyo Nyumba (Al Kaaba) ila ni kupiga miunzi na makofi. Basi onjeni adhabu kwa vile mlivyo kuwa mkikufuru.³⁵
- 36.** Hakika wale walio kufuru hutoa mali yao ili kuzuilia Njia ya Mwenyezi Mungu. Basi watayatoa, kisha yatakuwa juu yao majuto, na kisha watashindwa. Na wale walio kufuru watakusanywa kwenye Jahannam.³⁶
- 37.** Ili Mwenyezi Mungu apate kuwa pambanua walio waovu na walio wema, na kuwaweka waovu juu ya waovu wengine, na kuwarundika wote pamoja, na kuwatupa katika Jahannam. Hao ndio walio khasirika.³⁷
- 38.** Waambie wale walio kufuru: Wakikoma watasamehewa yaliyo kwisha pita. Na wakiyarudia basi imekwisha pita mifano ya wa zamani.³⁸
- 39.** Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayo yatenda.³⁹
- 40.** Na kama wakigeuka basi jueni kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Mola wenu, ni Mola Mwema na Msaidizi Mwema.⁴⁰
- 41.** NA JUENI ya kwamba ngawira mnayo ipata, basi khums (sehemu moja katika tano) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na wasafiri, ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyo yateremsha kwa mja wetu siku ya kipambanuo, siku yalipo kutana majeshi mawili. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.⁴¹

anawaakhirisha kwa alivyo wakadiria katika ujuzi wake kuwa wengi wao watakuja amini. Wao wakati huu wa sasa sio walenzi wa kuunusuru huo Msikiti Mtukufu, bali wao wameunajisi kwa kutia ibada ya masanamu ndani yake. Ama wa kuunusuru hakika ni Waumini, wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu. Lakini wengi katika washirikina hawajui Dini, wala hawajui cheo cha Nyumba hiyo Tukufu.

35 Na maombi yao kwenye Nyumba hii Tukufu (Al Kaaba) si chochote ila ni kupiga myunzi na makofi. Ilivyo kuwa hiyo ndiyo hali yenu, basi wacha mauti yakupatani, na yaonjeni katika uwanja wa vita, upate kubaidika ushirikina kutokana na Al Kaaba. Na kuuliwa huko kwenu ni kwa sababu ya ukafiri wenu.

36 Hakika hao wanao zipinga Ishara za Mwenyezi Mungu na wanamshirikisha na miungu mingine, hutoa mali yao ili wawazuie watu wasiifuate Imani ya Haki! Nao wataendelea kutoa hayo mali, kisha hayo mali, kwa kuwapotea bure bila ya pato walitakalo, yatawaletea majuto na machungu. Na katika uwanja wa mpambano watashindwa hapa duniani, na kisha watakusanywa wote katika Jahannam, wakibaki na ukafiri wao

37 Kwa kushindwa makafiri duniani na kuadhibiwa Motoni Akhera Mwenyezi Mungu anapambanua aliyे khabithi wa roho na vitendo na maneno, awe mbali na aliye mwema wa roho yake na moyo wake. Na awafanye wale waovu makhabithi wapandane wenyewe kwa wenyewe, huyu juu ya huyu, na awatie Motoni Siku ya Kiyama. Na hao washirikina mafisadi ndio wenye kukhasiri peke yao, duniani na Akhera.

38 Hakika juu ya vitisho hivi, mlango wa matarajio ungali wazi. Basi ewe Nabii wa rehema! Waambie hawa wapinzani kuwa wakikoma, wakaacha inadi yao na ushirikina wao, basi hapana shaka Mwenyezi Mungu atawasamehe vile vitendo vyao vilivyo kwisha pita. Na wakiendelea na upotovu wao, na wakarudia tena kukupigeni vita, basi mwendo wa Haki kwa walio tangulia umethibiti utakuwa ule ule, nao ni kuwa Haki lazima iushinde upotovu, pindi ikiwa wale watu wa Haki wakishika ut'iiifu na njia za ushindi.

39 Na endeleeni kuwapiga vita washirikina mpaka waache kuharibu itikadi za Waumini kwa kuwatesa na kuwaudhi. Wakiacha ukafiri na kuwaudhi Waumini, na wakamsafia Dini Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuvijua vitendo vyao, na atawalipa kwavyo.

40 Na wakiendelea na kupuza kwao na kuwaudhi Waumini, basi enyi Waumini, jueni ya kuwa nyinyi mko katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu, na huo ndio ulinzi wenye kupendeza na wenye nguvu kabisa. Na Yeye ndiye Mwenye kukunusuruni, na nusura yake ndio yenye nguvu zaidi na bora zaidi.

41 Na enyi Waislamu! Jueni kuwa katika mali ya makafiri mliyo yateka, hukumu yake ni kugawiwa mafungu matano. Fungu moja ni la Mwenyezi Mungu na Mtume, na jamaa zake Mtume, na mayatima, nao ni watoto wadogo wa Waislamu waliofiwa na baba zao nao ni mafakiri; na masikini, nao ni wale

42. Kumbukeni pale mlipo kuwa nyinyi kwenye ng'ambo ya karibu ya bonde, na wao wakawa ng'ambo ya mbali, na msafara ulipo kuwa chini yenu. Na ingeli kuwa mmeagana mngeli khitalifiana katika miadi. Lakini (mkakutana) ili Mwenyezi Mungu atimize jambo lilio kuwa lazima litendeke, kwa sababu aangamie wa kuangamia kwa dalili zilizo dhaahiri, na asalimike wa kusalimika kwa dalili zilizo dhaahiri. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.⁴²

43. Kumbuka alipo kuonyesha usingizini mwako kwamba wao ni wachache - na lau angeli kuonyesha kuwa ni wengi, mngeli ingiwa na woga, na mngeli zozana katika jambo hilo. Lakini Mwenyezi Mungu kakuvueni. Hakika Yeye ni Mwenye kuyajua yalio vifuani.⁴³

44. Na mlipo kutana akakuonyesheni machoni mwenu kuwa wao ni wachache, na akakufanyeni nyinyi ni wachache machoni mwao, ili Mwenyezi Mungu atimize jambo lilio kuwa liwe. Na mambo yote hurejzwa kwa Mwenyezi Mungu.⁴⁴

45. Enyi mlio amini! Mkikutana na jeshi, basi kueni imara, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu sana ili mpate kufanikiwa.⁴⁵

Waislamu wenye haja; na msafiri, naye ni mwenye kukatikiwa safari yake ya halali. Na yaliyo khusishwa katika hiyo sehemu moja katika tano kuwa ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume hukhusishwa kwa maslaha ya umma kama anavyo pasisha Mtume katika uhai wake, au, baada ya kufa kwake, Imam. Na yaliyo baki katika ile Khumsi watapewa walio kwisha tajwa. Ama sehemu nne nyengine katika ghanima (ngawira), na Aya ikanyamaza kimya juu yake, ni za wale walio pigana. Basi jueni hayo, na myajue ikiwa mmeuamini Mwenyezi Mungu kweli, na mmeziamini Ishara tulizo mteremshia mja wetu, Muhammad, za kumthibitisha na kumsaidia, siku ya Mpambanuo, tulipo pambanua baina ya ukafiri na Imani, nayo ndiyo siku lilipo kutana kundi lenu na kundi la makafiri katika Badri. Na Mwenyezi Mungu Mwenye kudra kubwa juu ya kila kitu aliwapa ushindi Waumini juu ya uchache wao, kuwashinda makafiri juu ya wingi wao.

42 Na kumbukeni mlipo kuwa bondeni ng'ambo hii ya karibu na Madina, na wao makafiri wako ng'ambo ile ya mbali, na msafara wenye bidhaa mlio kuwa mnautaka uko karibu zaidi nanyi upande wa baharini. Na lau kuwa mmepeana miadi ya kukutana kwa kupigana basi msinge wafikiana hivyo. Lakini Mwenyezi Mungu kapanga mkutane bila ya miadi, na bila ya kutaka wao, ili apate kutekeleza jambo ambalo katika ujuzi wake limekwisha thibiti litokee tu, wala hapana jengino. Jambo lenyewe ni kuwa vitokee vita vitavyo pelekea nyinyi mshinde na wao washindwe. Ipate kuondoka shaka - watekete wa kuteketea kwa hoja wazi ya kuonekana, nako ni kushindwa makafiri juu ya wingi wao; na wahuiki Waumini kwa hoja iliyo wazi, nako ni kushinda kulio toka kwa Mwenyezi Mungu kuwapa Waumini wachache. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na kujua. Haimfichikii kauli wala niya yoyote ya pande zote mbili.

43 Na kumbuka, ewe Mtume! Pale Mwenyezi Mungu alipo kufadhili kwa kukuonyesha usingizini ndoto ya kuwa hilo jeshi la maadui ni dogo, ili akutulizeni nyoyo muamini kuwa mtawashinda, kwa hivyo muwe imara kuwakaabili. Na lau angeli kuacheni muwaone wengi, bila ya kukuthibitisheni kwa ndoto hiyo, mngeli waogopa, na mkasita sita kupigana nao, na mngeli emewa, na mkazozana msonge mbele au mrudi. Lakini Mwenyezi Mungu amekuvueni na hayo, na akakuokoeni na matokeo yake, kwani hakika Yeye ni Mwenye kuyajua vyema yaliyomo ndani ya vifua vya watu.

44 Na kumbuka, ewe Mtume! Alipo kuonyeshemi Mwenyezi Mungu kuwa maadui zenu mnapo kutatana nao ni wachache katika macho yenu, kama alivyo waonyesha wao kuwa nyinyi ni wachache, na kwa kuwa tangu hapo wao wana ghururi ndani ya nafsi zao kuwa ni wengi, ili kila mmoja wenu awanie kupigana na mwenzie, na kwa hivyo yatimie aliyi kwisha yaamrisha Mwenyezi Mungu. Na ilikuwa hapana budi hayo yatimie. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio hurejea mambo yote ya ulimwengu. Halitendeki jambo ila alilo kwisha lihukumia na kuzitengeneza sababu zake.

45 Enyi mlio amini! Mkikutana na kikosi cha wapiganaji katika adui zenu, basi kuweni imara, wala msiwakimbie. Na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa kufuata uwezo wake, na ahadi yake ya kuwasaidia Waumini, mkikithirisha kumkumbuka na kumtaja pamoja na kuwa imara na kusubiri. Mkifanya hivyo ndio matarajio yenu ya kupata mafanikio yatapo timia.

46. Na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msizozane mkaingiwa woga, na zikapotea nguvu zenu. Na subirini. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri.⁴⁶

47. Wala msiwe kama wale walio toka majumbani mwao kwa fakhari na kujionyesha kwa watu, na wakawazuilia watu Njia ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ameyazunguka yote wanayo yafanya.⁴⁷

48. Na pale Shet'ani alipo wapambia vitendo vyao, na akawaambia: Hapana watu wa kukushindeni hii leo, na hali mimi ni mlinzi wenu. Yalipo onana majeshi mawili, akarudi nyuma, na akasema: Mimi si pamoja nanyi. Mimi naona msiyo yaona. Mimi namwogopa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.⁴⁸

49. Na walipo sema wanaafiki, na wale wenye ugonjwa nyoyoni mwao: Watu hawa dini yao imewadanganya. Na Mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Ametukuka, na Mwenye hikima.⁴⁹

50. Na laiti ungeli ona Malaika wanapo wafisha wale walio kufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao, na kuwaambia: Ionjeni adhabu ya Moto!⁵⁰

51. Hayo ni kwa sababu ya yale yaliyo kwisha tangulizwa na mikono yenu, na hakika Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja.⁵¹

52. Kama ada ya watu wa Firauni na walio kuwa kabla yao - walizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu. Basi Mwenyezi Mungu aliwashika kwa sababu ya madhambi yao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na mkali wa kuadhibu.⁵²

46 Na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika mambo mlio amrisha na mlio katazwa. Na wacheni kuzozana na kukhitalifiana. Hayo ndiyo yanayo pelekea kupoteza nguvu na kushindwa. Na vumilieni mkipata shida za vita. Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanao vumilia wakasubiri kwa kuwapa msaada na kuwaunga mkono, na kuwalipa malipo mema.

47 Wala msiwe kama wale walio toka kwenye majumba yao, nao wana ghururi (udanganyifu) kwa nguvu na neema walizo nazo, wakijifakhari na kujionyesha mbele za watu, wakitaka wasifiwe kwa ushujaa na ushindi, na wao huku wanapinga watu katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wanaupinga Uislamu. Na Mwenyezi Mungu amevizunguka vitendo vyao kwa ujuzi na uwezo. Na Yeye atakuja walipa duniani na Akhera.

48 Na kumbukeni, enyi Waislamu! Pale Shetani alipo kuja kuwazaini hawa washirikina kwa kuwaonyesha kuwa wayatendayo ni mazuri kwa uchochezi wake, akiwaambia: Hapana mtu ye yote anaye weza kuwashinda. Na akawahakikishia kuwa yeye atawalinda, na kuwanusuru! Yalipo kutana makundi mawili katika vita, vitimbi vyake na uchochezi wake ukavunjika. Akarejea nyuma, na akajitoa nao, akaogopa Mwenyezi Mungu asimuangamize. Na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

49 Na kumbuka ewe Mtume! Walipo sema wanaafiki miongoni mwa makafiri na wale wenye Imani dhaifu walipo kuoneni mmesimama imara: Hawa Waislamu wameghurika kweli na dini yao! Na hakika mwenye kumwakilisha Mwenyezi Mungu jambo lake, na akamuamini Yeye, na akamtegemea Yeye, basi hapana shaka kuwa Mwenyezi Mungu atamkifia amwondolee hamu yake, na atamnusuru na maadui zake. Kwani hakika Mwenyezi Mungu madaraka yake yana nguvu, naye ni Mwenye hikima katika mipango yake

50 Na lau kuwa unaona, ewe Mtume, kile kitisho kikubwa, kinacho wateremkia hawa makafiri, wakati ule Malaika wanapo wafisha na kuwang'oa roho zao, nao wakiwapiga mbele na nyuma, na wakiwaambia: Onjeni adhabu ya Moto kwa sababu ya vitendo vyenu viovu!!

51 Na hakika Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja wake kwa kuwaadhibu kwa madhambi waliyo yatenda. Bali huo ni uadilifu, kwa sababu hawawi sawa muovu na mwema. Basi kuadhibiwa kwake ni kwa vitendo viovu alivyo vitenda mwenyewe.

52 Hakika ada ya hawa washirikina, na shani yao katika ukafiri, ni kama shani ya Mafirauni na majabari wote walio baki walio kuwa kabla yao. Walizipinga Ishara za Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu aliwaadhibu kwa madhambi yao. Wala Yeye si mwenye kuwadhulumu. Hakika Mwenyezi Mungu ni

- 53.** Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu habadilishi kabisa neema alizo waneemesha watu, mpaka wao wabadilishe yaliyomo ndani ya nafsi zao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.⁵³
- 54.** Ni kama ada ya watu wa Firauni na walio kabla yao - walizikanusha Ishara za Mola wao Mlezi, basi tukawateketeza kwa madhambi yao. Na tukawazamisha watu wa Firauni. Na wote walikuwa wenye kudhulumu.⁵⁴
- 55.** Hakika vinyama vilio viovu kabisa mbele ya Mwenyezi Mungu ni wale wanao kufuru, basi hao hawaamini,⁵⁵
- 56.** Wale ambao miongoni mwao umepatana nao ahadi, kisha wanavunja ahadi yao kila mara, wala hawamchi Mungu.⁵⁶
- 57.** Basi ukiwakuta vitani wakimbize walio nyuma yao ili wapate kukumbuka.⁵⁷
- 58.** Na ukichelea khiana kwa watu fulani basi watupilie ahadi yao kwa usawa. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi makhaini.⁵⁸
- 59.** Wala wasidhanie wale walio kufuru kwamba wao wametangulia mbele. La, wao hawatashinda.⁵⁹
- 60.** Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi walio fungwa tayari-tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, na wengineo ambao hamwajui, lakini Mwenyezi Mungu anawajua. Na mkitoa chochote katika Njia ya Mwenyezi Mungu mtarudishiwa, na wala nyinyi hamtadhulumuwa.⁶⁰

Mwenye nguvu katika kutekeleza hukumu yake, na Mkali wa kumlipa anaye stahiki adhabu.

53 Na huu ni uadilifu katika kulipa, kwa sababu Mwenyezi Mungu hakika haibadilishi neema anayo waneemesha watu, kama vile neema ya amani, kutoonoka, na afya, mpaka wao wenyewe waigeuze hali yao na sababu zake! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyasikia wayasemayo, na Mwenye kuyajua wayatendayo.

54 Kama ilivyo kuwa ada yao na mtindo wao hawa katika kuzikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu na neema zake ni kama mtindo wa watu wa Firauni na walio watangulia, hali kadhaalika ada yao na shani yao katika kuendelea kuwakadhibisha Mitume wake, na dalili za Unabii wao, ni kama ada ya watu wa Firauni na walio kabla yao. Basi wamefanana hao katika kukanusha Ishara, na kuupinga Utume wa Mitume, na kuwakadhibisha, na kuendelea juu ya mwendo huo vile vile. Na kila mmoja Mwenyezi Mungu amentia mkononi kwa dhambi zake -wale kwa midharuba, na vimbunga, na kadhaalika; na watu wa Firauni kwa kuwazamisha. Na wote walikuwa ni madhaalimu wa nafsi zao. Kwa hivyo walistahiki adhabu iliyo wafika.

55 Hakika katika vyote vilio enea juu ya uso wa ardhi walio waovu mno mbele ya Mwenyezi Mungu katika hukumu yake na uadilifu wake, ni makafiri walio kakamia juu ya ukafiri wao.

56 Nao ni wale ulio fungamana nao kwa mikataba, nao wakawa hawaachi kuivunja kila mara; na watu hao ni Mayahudi ambao hawachelei utukufu wa Mwenyezi Mungu, wala hawakhofu kupatilizwa naye, wala adhabu yake.

57 Basi ewe Mtume! Ukiwakuta hawa wavunjao mapatano, na ukasadifiana nao katika vita nawe umeshinda, basi watishe baraabara kwa kuwapa adhabu ya kuwatia uchungu na kuwaogopesha wale walio nyuma yao, upate kuwafarikisha walio baki. Mateso haya ndiyo ya kuwakumbusha uovu wa kuvunja mapatano, na kuwazuia wenginewe wasitende kama hayo. (*Tazama Maelezo 8:57*)

58 Na ukiona alama za hao watu kutaka kuleta khiana kuvunja maagano yaliyo baina yako na wao, ikate njia yao wasiweze kukukhuni, kwa kuwatangazia wewe kuvunja hayo mapatano, mpaka walijue jambo lako, na wasiweze kukukhuni. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi makhaini, wala haridhii kuwa nyinyi msifike kwa sifa yao.

59 Wala wasidhani walio kufuru kuwa wamekwisha tangulia na wameiepuka adhabu ya kukhuni kwao na kwenda kinyume! Wao kabisa hawatamshinda Mwenyezi Mungu asiwazunguke na kuwatia nguvuni, bali Yeye peke yake ni Muweza, na atawalipa kwa nguvu zake na uadilifu wake.

60 Enyi Umma wa Kiislamu! Tayarisheni kila muwezavyo nguvu za vita za namna zote kwa ajili ya kujizatiti kwa ajili ya kupigana, na wekeni askari walinzi na farasi wao mipakani na kando kando ya

61. Na wakielekea amani nawe pia elekea, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua.⁶¹
62. Na wakitaka kukukhadaa basi Mwenyezi Mungu atakutosheleza. Kwani Yeye ndiye aliye kuunga mkono kwa nusura yake na kwa Waumini.⁶²
63. Na akaziunga nyoyo zao. Na lau wewe ungesi toa vyote viliomo duniani usingeli weza kuziunga nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye waunganisha. Hakika Yeye ndiye Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima.⁶³
64. Ewe Nabii! Mwenyezi Mungu anakutoshelezea wewe na Waumini walio kufuata.⁶⁴
65. Ewe Nabii! Wahimize Waumini wende vitani. Wakiwapo kati yenu ishirini wanao subiri watawashinda mia mbili. Na wakiwapo kati yenu mia watawashinda elfu moja katika walio kufuru. Kwa sababu wao ni watu wasio fahamu.⁶⁵
66. Sasa Mwenyezi Mungu amekupunguzieni, na anajua kuwa upo udhaifu kwenu. Kwa hivyo wakiwa wapo watu mia moja kati yenu wenye kusubiri watawashinda mia mbili. Na wakiwapo elfu moja watawashinda elfu mbili, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wenye kusubiri.⁶⁶

nchi, ili kwa hivi mjitayarisha na ulinzi mwatie kiwewe adui za Mwenyezi Mungu na adui zenu miongoni mwa hao makafiri ambao wamo kungojea likupateni jambo. Na pia mpate kuwatishia wenginewe ambao nyinyi hamwajui hivi sasa, lakini Mwenyezi Mungu anawajua, kwani hapana jambo linalo jificha kwake. Na kila mnacho kitoa kwa kuzitayarisha nguvu zenu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi Yeye atakulipeni malipo ya kutosha, bila ya kupunguka hata chembe katika mnayo stahiki katika fadhila ya Mola wenu Mlezi. (*Tazama Maelezo 8:60*)

61 Maadui wakielekea kutaka amani na kuacha uadui wao, basi nawe ewe Mtume, elekea kwenye amani. Kwani vita sio lengo, bali wewe unakusudia kujilinda tu na uadui wao na upinzani wao kupinga wito wako. Basi kubali amani, na umtegemee Mwenyezi Mungu, wala usikhofu vitimbi vyao na njama zao! Yeye *Subhanahu* ni Mwenye kuzisikia njama zao, ni Mwenye kuijua mipango yao. Hapana kinacho fichikana kwake.. (*Tazama Maelezo 8:61*)

62 Ikiwa hao maadui wanataka kukukhadaa na kukufanyia ujanja kwa hivyo kuonyesha kuwa wanataka amani, basi Mwenyezi Mungu anakutosheleza kukulinda na vitimbi vyao kwa kila upande. Kwani Yeye alikwisha tangulia kukuunga mkono kwa kukupa ushindi pale alipo kutengeneza sababu zilizo onekana na za siri za kutia imara nyoyo za Waumini katika Wahajiri, wahamiaji walio toka Makka, na Ansari, wasaidizi wa Madina.

63 Na Mwenyezi Mungu akawaweka pamoja kwa mapenzi baada ya mtafaruku na uadui, hata wakawa marafiki mbele yako, wakizisabilia roho zao na mali yao kwa ajili ya wito wako. Na wewe hata ungesi toa mali yote na vitu vyote vya nafuu viliomo duniani kwa ajili ya kuwaunga pamoja huku, usinge weza kuyapata hayo. Kwa sababu nyoyo zimo katika mkono wa Mwenyezi Mungu, na Yeye ndiye aliye waunganisha, kwa kuwaongoa kwenye Imani na mapenzi na udugu. Hakika Yeye Mtukufu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda. Anawapangia waja wake kwa mujibu wa manufaa yao.

64 Ewe Nabii! Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mwenye kukudhamini wewe na wenye kukufuata miongoni mwa Waumini katika kila jambo lenye maana kwenu.

65 Ewe Nabii! Wahimize Waumini wende vitani kwa ajili ya kulinyanyua Neno la Mwenyezi Mungu, na wapendezeshe kwa yatayo wafwatia katika kheri ya dunia na Akhera watayo ipata, ili nafsi zao ziingie nguvu. Nayo ikiwa wapo kati yenu watu ishirini walio shikamana na Imani na subira na ut'iifu, basi watawashinda makafiri mia mbili. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio fahamu ukweli wa mambo, kwani hawana Imani, wala subira, wala tamaa ya kupata thawabu.

66 Ilivyo kuwa ni waajibu wenu enyi Waumini, kusubiri mnapo kutana na maadui zenu katika hali ya kuwa mna nguvu, ijapo kuwa wamekuzidini mara kumi, sasa Mwenyezi Mungu amekuruhusini katika hali isiyo kuwa ya nguvu, kuwa mvumilie ikiwa adui kakuzidini mara mbili basi. Hayo ni kwa kukujua kwake kuwa hamna nguvu nyingi, kwa hivyo mmefanyiwa wepesi na mmesahilishiwa, baada ya kuwa heba ya Uislamu imeingia katika nafsi za makafiri. Kwa hivyo mkiwa nyinyi ni wapiganaji mia wenye kusubiri mnaweza kuwashinda makafiri mia mbili. Na mkiwa elfu moja mtawashinda elfu mbili, kwa Mwenyezi Mungu kupenda na kusaidia. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wenye kusubiri kwa nusura

67. Haimfalii Nabii yeyote kuwa na mateka mpaka awe ameshinda baraabara katika nchi. Mnataka vitu vya dunia, na Mwenyezi Mungu anataka Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu Mwenye hikima.⁶⁷

68. Lau isingeli kuwa hukumu iliyo kwisha tangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu ingeli kupatani adhabu kubwa kwa vile mlivyo chukua.⁶⁸

69. Basi kuleni katika mlivyo teka, ni halali na vizuri, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.⁶⁹

70. Ewe Nabii! Waambie mateka waliomo mikononi mwenu: Kama Mwenyezi akiona kheri yoyote nyoyoni mwenu atakupeni bora kuliko vilivyo chukuliwa kwenu, na atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.⁷⁰

71. Ikiwa wanataka kukufanyia khiana, wao walikwisha mfanyia khiana Mwenyezi Mungu kabla yake, na Yeye akakuwezesha kuwashinda. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.⁷¹

72. Hakika wale walio amini na wakahama na wakapigania Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao, na wale walio toa mahala pa kukaa, na wakanusuru, hao ni marafiki na walinzi wao kwa wao. Na wale walio amini lakini hawakuhama, nyinyi hamna waajibu wa ulinzi kwao hata kidogo mpaka wahame. Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia, isipo kuwa juu ya watu ambao yapo mapatano baina yenu na wao. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yatenda.⁷²

yake na kuunga mkono kwake.

67 Haimfalii Nabii yeyote kukamata mateka, au kuchukua fidia, au kutoa bure msamaha, mpaka ashinde, na maadui waone wameshindwa, na wawe wamepata pigo kubwa hata kuwa hawawezi tena kupigana katika nchi. Lakini, nyinyi jamaa wa Kiislamu, mmefanya haraka katika Vita vya Badri kukamata mateka kabla hamjatamakani mkawa imara katika nchi. Mnatafuta manufaa ya dunia, na Mwenyezi Mungu anataka Akhera, kwa kutukuzwa Neno la Haki, na lisikushughulisheni la dunia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda. Hukupangieni mambo yenu kwa mujibu wa faida yenu.

68 Ingeli kuwa hapana hukumu iliyo kwisha tangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu ya kumsamehe mwenye kujitahidi japo kuwa amekosa, basi ingeli kupatani adhabu kubwa kwa papara mliyo ifanya.

69 Basi sasa tumieni mlicho kipata katika fidia kwa kuwa ni halali kwenu, wala si uchumi muovu. Na mcheni Mwenyezi Mungu katika mambo yenu yote. Hakika Mwenyezi Mungu ni mkubwa wa kusamehe na kumrehemu amtakaye katika waja wake pindi akirejea.

70 Ewe Nabii! Waambie hao mateka walio angukia mikononi mwenu: Ikiwa katika nyoyo zenu ipo kheri anayo ijua Mwenyezi Mungu, Yeye atakupeni yaliyo bora zaidi kuliko hicho walicho kichukua Waumini, na atakusameheni ushirikina wenu na madhambi mliyo kuwa nayo. Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghfira na rehema kwa mwenye kutubia madhambi yake.

71 Na pindi wakitaka kukukhuni, kwa vile baadhi yao walivyo onyesha kumili kwenye Uislamu, pamoja na nyoyo zao kupenda kukufanyia khiana makusudi, wewe usivunjike moyo. Mwenyezi Mungu atakupua uwezo juu yao. Kama hapo kwanza walipo mkhini Mwenyezi Mungu kwa kumfanyia wenzi na washirika wa kuwaabudu, na wakaikufuru neema yake, na Yeye aliwaweza kwa kukupa ushindi juu yao katika Badri, juu ya kuwa jeshi lako ni dogo na lao ni kubwa. Na Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu, Mwenye ushindi, Muendeshaji kwa hikima yake, aliwathibitisha wakawa na nguvu waja wake Waumini kwa nusura yake.

72 Hakika walio isadiki Haki na wakaikubali hukumu yake, wakahama Makka, wakapigana Jihadi kwa mali yao na roho zao, na wale walio wapa makaazi wakimbizi ugenini, wakamsaidia Mtume wa Mwenyezi Mungu, wanapigana vita na wale wanao wapiga vita. Wanamfanyia uadui anao wafanyia uadui. Wao kwa wao wanasaidia kuunga mkono Haki, na kutukuza Neno la Mwenyezi Mungu. Na wale wasio hama, haijathibiti kupata ulinzi na msaada wa Waumini, mpaka wahajiri. Lakini wakitakeni muwanusuru na wanao wakandamiza katika Dini, basi wanusuruni. Wakitakeni muwasaidie dhidi ya watu ambao mna mapatano nao, na wala hawakuvunja mapatano hayo, basi msiwakubalie. Na Mwenyezi Mungu anayaona myatendayo, hana kinacho fichika kwake. Basi simameni kwenye mipaka yake msije mkatumbukia katika adhabu yake.

73. Na wale walio kufuru ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Msipo fanya hivi itakuwako fitna katika nchi na fisadi kubwa.⁷³

74. Na walio amini wakahama na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na walio toa mahala pa kukaa na wakanusuru, hao ndio Waumini wa kweli. Watapata msamaha wa Mwenyezi Mungu na kuruzukiwa kwema.⁷⁴

75. Na watakao amini baadaye na wakahajiri, na wakapigana Jihadi pamoja nanyi, basi hao ni katika nyinyi. Na jamaa wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe zaidi katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.⁷⁵

73 Na walio kufuru wao ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Na wao husaidiana kwa mambo ya upotovu, na wanaungana mkono kukufanyieni nyinyi uadui. Basi nyinyi msifanye nao urafiki. Mkikhaalifu, yaani mkenda kinyume na haya mkawafanya ni wenzenu itaingia fitna katika safu zenu, na utakuwa uharibifu mkubwa katika nchi.

74 Na walio amini, na wakahajiri, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na walio wapa makaazi, na wakaisaidia Haki na Neno la Mwenyezi Mungu - hao ndio walio na Imani ya kweli. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu atawasamehe, na watapata riziki kubwa duniani na Akhera.

75 Na walio amini baada ya wale wa mwanzo, na mwishoe wakahama nao, na wakapigana Jihadi pamoja na walio tangulia, basi hao ni katika nyinyi, kwa mkusanyo wa Muhaajirina (Walio hama Makka) na Ansari (walio msaidia Mtume, watu wa Madina). Hao wanastahiki ulinzi na haki kama zilioopo baina ya nyinyi kwa nyinyi. Na walio kuwa wame nasibiana katika Waumini - juu ya urafiki wa Imani -wana urafiki zaidi wa kuwa ni jamaa. Basi hao wanazidiana katika mapenzi, na mali, na kusaidiana, na kuungana mkono. Na Mwenyezi Mungu ameyabainisha hayo katika Kitabu chake. Naye ni Mwenye kujua kila kitu.

Sura 9 - At-Tawba

Utangulizi

Suratut Tawba iliteremka Madina katika mwaka wa tisa wa Hijra, yaani miaka tisa baada ya Mtume s.a.w. kuhamia Madina. Akaichukua Sura hii Ali bin Abi Talib r.a. kuwapelekea Waislamu katika Hija na akawasomea. Na amir, yaani mwongozi, wa Hija hiyo alikuwa Abu Bakr Assidiq r.a. Na Aya zake ni 129. Imeanzia kwa kujitenga Mwenyezi Mungu Mtukufu na washirikina. Na kwa hivyo ikaitwa pia Sura ya Baraaah, yaani kujitenga, kutokuwa na dhima, kutokuwa na jukumu. Na baada ya hayo ikataja utakatifu wa miezi mitakatifu, na ahadi za washirikina, na ipasavyo kutimiza ahadi nao ikiwa wao hawajaivunja. Na mwenye kuvunja ahadi yapasa kupigana naye. Na baada ya hayo ikabainisha kuwa kiini cha kutaka kumkaribia Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kumuamini Yeye. Na Imani haikamiliki ila akiwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapendwa na Waumini kuliko kila kitu. Naye *Subhanahu* ametaja kuwa kujiona una nguvu ndio kunapelekea kuwa mbali ushindi, na akaashiria mfano wa vita vya Hunayni. Katika Sura hii wamepigwiwa marufuku washirikina wasiingie katika Msikiti Mtakatifu wa Makka, kwa kuwa wao ni najisi!

Na katika Sura hii imetajwa kupasa kuwapiga vita Mayahudi na Wakristo mpaka watoe jizya, kodi ya kichwa, na imebainishwa idadi ya miezi mitakatifu. Na humu imebainishwa dharura ya kutoka kwenda vitani kila vikinadiwa bila ya kulegalega. Na humo imeashiriwa hukumu ya wanao bakia nyuma, na walemevu wasio weza kwenda kupigana, na imebainishwa hali ya wanaafiki ambao wanatafuta fitna kila wakati vinapo nadiwa vita. Na Mwenyezi Mungu akataja wanaafiki wanavyo watendea Waumini wakati wa salama na vita.

Katika Sura hii iko amri ya kukata iliyo tangazwa kuwatia adabu wanaafiki. Nayo ni kuwa Mtume s.a.w. asimsalie yeyote katika wanaafiki akifa. Naye *Subhanahu* ametaja udhuru unao mstahikia mtu kubaki nyuma asende vitani. Na pia *Subhanahu* ameeleza hali ya wale mabedui walio dhihirisha kuingia katika Uislamu, au wakafuata hukumu zake, baada ya kuwa Uislamu umepata nguvu. Na akaeleza kuwa hao mabedui wako kando kando ya Madina.

Na baada ya hayo ametaja hali za watu kwa mnasaba wa Imani. Na akataja khabari ya Msikiti wa Madhara walio ujenga wanaafiki ili upuuzwe Msikiti alio ujenga Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. Kisha *Subhanahu* akataja sifa za Waumini walio wakweli katika Imani yao, na toba ya wale walio mkhalifu Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w., na Mwenyezi Mungu akakubali toba hiyo, kama alivyo taja *Subhanahu wa Taa'la* hali za watu katika kuzipokea Aya za Qur'ani zinapo teremka. Na *Subhanahu wa Taala* akakhitimisha Sura hii kwa kusema kuwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amemteua Muhammad kwa kumpa Utume, na kwamba yeye hawataki shida hao alio tumwa kwao, na kwamba yeye ni mpole na mwenye huruma kwao, na kwamba ikiwa wakigeuka basi Mwenyezi Mungu anamtosheleza. (Angalia: Sura hii peke yake ndiyo haianzii kwa Bismillahi, Kwa Jina la Mwenyezi Mungu.)

*** **

1. Huku ni kujitoa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwenye jukumu la maagano na mlio ahidiana nao katika washirikina.¹
2. Basi tembeeni katika nchi miezi mine, na jueni kwamba nyinyi hamwezi kumshinda Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu ndiye anaye wahizi makafiri.²
3. Na ni tangazo kutokana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa wote siku ya Hija Kubwa kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawana jukumu lolote kwa washirikina. Basi mkitubu itakuwa kheri kwenu, na mkigeuka basi jueni kuwa nyinyi hamumshindi Mwenyezi Mungu. Na wabashirie makafiri kuwa watapata adhabu chungu.³
4. Isipo kuwa washirikina ambao mliahidiana nao kisha wasikupunguzieni chochote, wala hawakumsaidia yeyote dhidi yenu, basi hao watimizieni ahadi yao mpaka muda wao. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wacha-Mungu.⁴
5. Na ikisha miezi mitukufu basi wauweni washirikina popote mwakutapo, na washikeni na wazungukeni, na wavizieni katika kila njia. Lakini wakitubu, wakashika Sala, na wakatoa Zaka, basi waachilieni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.⁵
6. Na ikiwa mmoja wapo katika washirikina akikuomba ulinzi, basi mpe ulinzi apate kusikia maneno ya Mwenyezi Mungu. Kisha mfikishe pahala pake pa amani. Haya ni kwa kuwa hao ni watu wasiojua kitu.⁶
7. Itakuwaje iwepo ahadi na washirikina mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya Mtume wake, ila wale mlio ahidiana nao kwenye Msikiti Mtakatifu? Basi maadamu wanakwenda nanyi sawa, nanyi pia nendeni sawa nao. Hakika Mwenyezi Mungu

1 Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanajitoa katika dhima, wala jukumu lolote, na wale washirikina mlio peana nao ahadi, na wao wakavunja hayo mlio ahidiana nao.

2 Basi nyinyi washirikina, mna amani kwa muda wa miezi mine, kuanzia tangazo hili, mzunguke mtakako katika muda huu. Lakini jueni kuwa popote mlipo nyinyi mko chini ya utawala wa Mwenyezi Mungu, na nyinyi hamuwezi kumshinda Yeye. Na mjue kuwa Mwenyezi Mungu amewaandikia hizaya iwapate hao wanao pinga.

3 Na hili ni Tangazo linalo toka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kuwatangazia watu wote wanapo jumuiika siku ya Hija Kubwa ya kwamba:- Hakika Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanajitoa katika dhima, au jukumu, yoyote katika mapatano na washirikina walio fanya khiana. Basi enyi washirikina, mlio vunja ahadi! Mkirudi mkaacha kumshirikisha Mwenyezi Mungu, itakuwa kheri kwenu hapa duniani na kesho Akhera. Lakini mkipuza na mkabakia hivyo hivyo mlivyo, basi jueni kuwa nyinyi mngali chini ya utawala wa Mwenyezi Mungu. Ewe Mtume! Waonye makafiri wote kuwa ipo adhabu kali yenye uchungu.

4 Ama wale washirikina mlio ahidiana nao na wakatimiza ahadi zao, wala hawakuacha chochote katika hayo, wala hawakumsaidia yeyote dhidi yenu, basi watimizieni ahadi zao mpaka mwisho na mzihishimu... Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wacha-Mungu wenye kutimiza ahadi zao.

5 Ukimalizika muda wa amani, yaani miezi mine, basi wauweni washirikina walio vunja ahadi katika kila pahala. Na watieni nguvuni, wazungukeni kwa kuwafungia njia, na wavizieni katika kila njia. Wakitubu wakaacha ukafiri wao, na wakafuata hukumu za Uislamu, kwa kushika Sala, na kutoa Zaka, basi nyinyi hamna sababu ya kuwashambulia, kwa kuwa wamekwisha ingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mkubwa wa Kusamehe kwa anaye tubu, na Mwenye rehema kunjufu kwa waja wake.

6 Ewe Mtume! Mmoja wapo katika washirikina ulio amrisha uwapige vita, akikutaka amani ili apate kusikia wito wako, basi mpe amani mpaka asikie maneno ya Mwenyezi Mungu. Akiingia katika Uislamu basi huyo ni mwenzenu. Na akitoingia mpeleke mpaka afike pahala pa amani kwake. Na haya ya kumpa ulinzi na amani mwenye kuomba ili asikie maneno ya Mwenyezi Mungu ni kwa sababu ya ule ujinga wake wa kutoujua Uislamu ulio kwisha dhihiri, na ile hamu yake ya kutaka kuujua.

huwapenda wachamngu.⁷

8. Itakuwaje! Nao wakikushindeni hawatazami kwenu udugu wala ahadi. Wanakufurahisheni kwa midomo yao tu, na nyoyo zao zinakataa hayo. Na wengi wao ni wapotovu.⁸

9. Wamenunua thamani ndogo kwa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakazuilia watu na Njia yake. Hakika hao ni maovu waliyo kuwa wakiyatenda.⁹

10. Hawatazami kwa Muumini udugu wala ahadi; basi hao ndio warukao mipaka.¹⁰

11. Basi wakitubu na wakashika Sala na wakatoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika Dini. Na tunazichambua Aya kwa watu wajua.¹¹

12. Na wakivunja viapo vyao baada ya kuahidi kwao, na wakatukana Dini yenu, basi piganeni na waongozi wa ukafiri. Hakika hao hawana viapo vya kweli. Huenda (kwa hayo) wakaacha.¹²

13. Je, hamtapigana na watu walio vunja viapo vyao na wakawa na hamu ya kumfukuza Mtume, nao ndio walio kuanzeni mara ya kwanza? Je, mnawaogopa? Basi Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi mumwogope, ikiwa nyinyi ni Waumini.¹³

14. Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awahizi na akunusuruni muwashinde, na avipoze vifua vya kaumu ya Waumini.¹⁴

15. Na aondoe hasira ya nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu humkubalia toba ya amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.¹⁵

7 Itakuwaje hawa washirikina, wanao vunja ahadi mara kwa mara, wawe na ahadi ya kuhishimiwa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya Mtume wake? Basi msichukue ahadi zao, ila wale katika kabila za Kiarabu mlio ahadiana nao kwenye Msikiti Mtakatifu, na kisha wakasimama sawa kwenye ahadi yao. Basi nanyi simameni sawa juu ya ahadi yenu maadamu wao wamesimama sawa. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wenye kumt'ii Yeye na wenye kutimiza ahadi zao.

8 Vipi nyinyi mtalinda ahadi zao nao ni watu ambao wakikuwezeni wanawasaidia maadui zenu dhidi yenu? Hawataacha fursa ya kukumalizeni bila ya kujali ujamaa (udugu) wala mapatano. Na watu hao hukudanganyeni kwa maneno yao yaliyo pakwa asali, na nyoyo zao zimekunja kwa kukuchukieni. Na wengi wao wametokana na Haki, ni wenye kuvunja ahadi.

9 Wamezitupa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakazibadilisha hizo kwa machache yasiyo dumu ya kidunia, na wakazuia watu wasiingie katika Dini ya Mwenyezi Mungu. Hakika wafanyayo watu hawa ni mabaya!

10 Hiyo ndiyo hali ya ukafiri wao. Hawahishimu ujamaa wala ahadi katika kuamiliana na Muumini. Shani ya watu kama hao ni kufanya uadui tu. Hayo ndiyo maradhi yao yasio wabanduka!

11 Wakitubia, wakaacha ukafiri wao, na wakashika hukumu za Uislamu, kwa kushika Sala, na kutoa Zaka, basi wanakuwa ni ndugu zenu katika Dini. Haki yao kama haki yenu. Jukumu lao kama jukumu lenu. Na Mwenyezi Mungu anazibainisha Aya hizi kwa watu wanao nafiika na ilimu.

12 Na pindi wakivunja ahadi zao baada ya kwisha zikubali, na wakaendelea kuitukana Dini yenu, basi wapigeni vita wakuu wa upotovu na walio pamoja nao, kwani hao hawana ahadi wala dhima, ili wapate kuacha ukafiri wao.

13 Enyi Waumini! Kwa nini msikimbilie kwenda vitani kuwapiga vita washirikina walio vunja mapatano yenu mara kwa mara, na wao walikuwa wakijihimu kumfukuza Mtume Makka na kumuua, na wao tena ndio walio kuanzeni kukuteseni na kukufanyieni uadui tangu mwanzo? Je, mnawaogopa? Msiwaogope! Mwenyezi Mungu tu peke yake ndiye anaye stahiki nyinyi mumwogope, kama nyinyi ni wakweli katika Imani yenu.

14 Enyi Waumini, piganeni nao! Mwenyezi Mungu atawaonjesha adhabu itokayo mikononi mwenu, na atawadhalilisha na atakupeni ushindi juu yao. Na kwa kuwashinda hao, na kuunyanyua utukufu wa Uislamu, Mwenyezi Mungu atayapoza machungu yaliyomo katika vifua vya Waumini, yaliyo fichikana na yaliyo dhiri, wakati wote walipo kuwa wakipata maudhi ya makafiri.

15 Na Mwenyezi Mungu atazijaza nyoyo za Waumini furaha ya kushinda baada ya kuwa na hamu na khofu, na atawaondoe hasira, na Mwenyezi Mungu atapokea toba ya amtakaye kumkubalia katika wao.

16. Je, mlidhani kuwa mtaachwa tu, bila ya Mwenyezi Mungu kuwajuulisha wale walio pigana Jihadi kati yenu, na wala hawakumfanya mwendani wao isipo kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Waumini wenziwe? Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayo yatenda.¹⁶

17. Haiwi kuwa makafiri ndio waamirisha misikiti ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudishia wenyewe ukafiri. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika, na katika Moto watadumu.¹⁷

18. Hakika wanao amirisha misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanao muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na wakashika Sala, na wakatoa Zaka, na wala hawamchi ila Mwenyezi Mungu. Basi huenda hao wakawa katika waongofu.¹⁸

19. Je, mnafanya kuwanyweshwa maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.¹⁹

20. Wale walio amini, na wakahama, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao, hao wana cheo kikubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye kufuzu.²⁰

21. Mola wao Mlezi anawabashiria rehema zitokazo kwake, na radhi, na Bustani ambazo humo watapata neema za kudumu.²¹

22. Watadumu humo milele. Hakika kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo makubwa.²²

Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa ujuzi kwa mambo yote ya waja wake, ni Mkuu wa hikima katika anayo waamirisha.

16 Enyi Waumini! Msidhani kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuacheni hivi hivi bila ya kukutieni mtihanini kwa Jihadi na mfano wa hayo. Ndio mwendo wake Mwenyezi Mungu kufanya mitihani, upate dhihiri ujuzi wake kwa wale kati yenu wanao pigana Jihadi, wenye ikhlasi (yaani nyoyo safi), na wala hawawafanyi marafiki, wendani na walinzi, isipo kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Waumini wenzao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua vyema vitendo vyenu vyote, na atakulipeni kwavyo.

17 Hawawi washirikina ndio wenye kufaa kuamirisha misikiti ya Mwenyezi Mungu, na hali wao wangali kuendelea na ukafiri wao, na wanautangaza khasa! Vitendo vyao washirikina havitiwi hisabuni, wala hawatolipwa thawabu kwavyo! Wao ni wenye kudumu Motoni Siku ya Kiyama.

18 Lakini wanao amirisha misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wenye kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja peke yake, na wakasadiki kuwapo kufufuliwa na kulipwa, na wakatimiza Sala kama itakikanavyo, na wakatoa Zaka ya mali yao, na wala hawamwogopi ila Mwenyezi Mungu peke yake. Na hao ndio wanao tarajiwa kuwa mbele ya Mwenyezi Mungu waongofu wa kufuata Njia Iliyo Nyooka.

19 Haifalii kuwafanya washirikina wanao wanyweshwa maji Mahujaji, na wakauamirisha Msikiti Mtakatifu (wa Makka), katika cheo kama cha wanao muamini Mwenyezi Mungu Mmoja, na wakasadiki kufufuliwa na kulipwa kwa wayatendayo, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Hao si makamu mamoja mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi kwenye Njia ya kheri watu ambao wameshikilia kujidhulumu wenyewe kwa ukafiri wao, na wakawadhulumu wengineo kwa maudhi yasio kwisha.

20 Wale walio sadiki kuwa Mwenyezi Mungu ni Mmoja, na wakauhama mji wa ukafiri kuendea mji wa Uislamu, na wakavumilia mashaka ya Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa kutoa mali yao na roho zao, hao wana cheo kikubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu, kuliko wengineo wasio na sifa hizi. Na hawa ndio wenye kufuzu, kuzipata thawabu za Mwenyezi Mungu na ukarimu wake.

21 Na hao Mwenyezi Mungu Mtukufu anawabashiria rehema kunjufu itakayo waenea, na atawakhusisha radhi zake, na hayo ndiyo malipo makuu. Na Siku ya Kiyama atawatia katika Mabustani, na humo watapata neema zenye kuthibiti na kudumu.

22 Na wao watadumu huko Peponi hawatoki. Na hakika kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo makubwa, na thawabu nyingi.

23. Enyi mlio amini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi vyenu ikiwa wanastahabu ukafiri kuliko Imani. Na katika nyinyi atakaye wafanya hao ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhaalimu.²³

24. Sema: Ikiwa baba zenu, na wenenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyo yachuma, na biashara mnazo ogopa kuharibika, na majumba mnayo yapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Jihadi katika Njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu.²⁴

25. Hakika Mwenyezi Mungu amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Hunayni ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni kitu. Na ardhi ikawa dhiki kwenu juu ya upana wake. Kisha mkageuka mkarudi nyuma.²⁵

26. Kisha Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya Waumini. Na akateremsha majeshi ambayo hamkuyaona, na akawaadhibu wale walio kufuru. Na hayo ndiyo malipo ya makafiri.²⁶

27. Kisha baada ya hayo Mwenyezi Mungu atawasamehe awatakao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.²⁷

28. Enyi mlio amini! Hakika washirikina ni najsi, kwa hivyo wasiukaribie Msikiti Mtakatifu baada ya mwaka wao huu. Na ikiwa mnakhofia umasikini, basi Mwenyezi Mungu atakutajirisheni kwa fadhila yake akipenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.²⁸

29. Piganeni na wasio muamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho, wala hawaharimishi alivyo harimisha Mwenyezi Mungu na Mtume, wala hawashiki Dini ya Haki, miongoni mwa walio pewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa khiari yao, hali

23 Enyi Waumini! Msiwafanye baba zenu, na watoto wenu, na ndugu zenu, na jamaa zenu, na wake zenu, ndio wasaidizi wenu wa kukunusuruni maadamu wanapenda ukafiri, na wanaufadhilisha kuliko Imani. Na wenye kutaka manusura kwa makafiri, ndio hao walio iwacha Njia Iliyo Nyooka.

24 Ewe Mtume! Waambie Waumini: Ikiwa baba zenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyo yachuma, na biashara mnazo khofu zisibwage, na majumba mnayo starehea kuyakaa, mnayapenda zaidi kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume na Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, hata mkaacha kumuunga mkono Mtume, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu akuleteeni hukumu yake na adhabu yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi wenye kutoka kwenye mipaka ya Dini yake.

25 Hakika Mwenyezi Mungu amekunusuruni na maadui zenu mara nyingi katika vita kwa nguvu ya Imani yenu. Na mlipo ghurika na wingi wenu katika vita vya Hunayni, kwanza Mwenyezi Mungu alikuachieni wenyewe. Wingi wenu usikufaeni kitu. Adui akakushindeni, na kwa shida ya kufazaika mkaiona ardhi kuwa ni nyembamba. Msiweze kupata njia ya kupigana wala kuokoka kwa murwa. Wengi wenu wakawa hawana njia ya kuepuka ila kukimbia. Mkakimbia kwa kushindwa, na mkamuacha Mtume na Waumini wachache tu. (*Tazama Maelezo 9:25*)

26 Tena mkapata himaya ya Mwenyezi Mungu. Akateremsha utulivu juu ya Mtume wake, na akaujaza utulivu katika nyoyo za Waumini, na akakuungeni mkono kwa Malaika, jeshi lake, walio tia imara miguu yenu. Nanyi hamkuwaona Malaika hao...Na Mwenyezi Mungu akawaonjesha maadui zenu machungu ya kushindwa. Na hayo ndiyo malipo ya makafiri duniani.

27 Kisha Mwenyezi Mungu atakubali toba ya amtakaye katika waja wake, na amsamehe dhambi zake, pindi akirejea kwa usafi wa moyo. Na Mwenyezi Mungu ni Mkubwa wa kusamehe, Mkuvunjufu wa kurehemu.

28 Enyi Waumini! Washirikina kwa sababu ya ushirikina wao wamejinajisi nafsi zao, nao wamepotea katika itikadi. Msiwaachilie kuingia Msikiti Mtakatifu baada ya mwaka huu (9 Hijra). Mkichelea ufakiri kwa kukatika biashara Mwenyezi Mungu atakupeni badala yake, na atakutoshelezeni kwa fadhila yake akipenda. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua mambo yenu yote, na Mwenye hikima katika mipango yake.

wamet'ii.²⁹

30. Na Mayahudi wanasema: Uzeir ni mwana wa Mungu. Na Wakristo wanasema: Masihi ni mwana wa Mungu. Hiyo ndiyo kauli yao kwa vinywa vyao. Wanayaiga maneno ya walio kufuru kabla yao. Mwenyezi Mungu awaangamize! Wanageuzwa namna gani hawa!³⁰

31. Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrisha isipo kuwa wamuabudu Mungu Mmoja, hapana mungu ila Yeye. *Subhanahu*, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo.³¹

32. Wanataka kuizima Nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, na Mwenyezi Mungu anakataa ila aitimize Nuru yake ijapo kuwa makafiri watachukia.³²

33. Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya Haki ipate kushinda dini zote, ijapo kuwa washirikina watachukia.³³

34. Enyi mlio amini! Hakika wengi katika makuhani na wamonaki wanakula mali za watu kwa baat'ili na wanazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu.³⁴

35. Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji

29 Enyi mlio amini! Wapigeni vita makafiri katika Watu wa Kitabu wasio muamini Mwenyezi Mungu kwa Imani iliyo sawa, wala hawakiri kuwa kuna kufufuliwa na kulipwa, wala hawayashiki aliyo yakataza Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala hawaishiki Dini ya Haki, nayo ni Uislamu. Wapigeni vita mpaka waamini, au watoe Jizya, nao wamenyenyekea na wat'iifu, si wenye kuasi, wasaidie katika kujenga mfuko wa Kiislamu. (*Tazama Maelezo 9:29*)

30 Mayahudi wameacha Tawhidi, ya kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja pekee, na wakasema kuwa Uzair ni mwana wa Mungu! (Mayahudi wa Arabuni tu ndio walimfanya Uzair ni mwana wa Mungu.) Na Wakristo nao wakaacha Imani ya Mungu Mmoja vile vile, wakasema: Masihi ni mwana wa Mungu!! Na kauli yao hii ni ya uzushi, wanakariri kwa vinywa vyao, wala hayakuletwa hayo na Kitabu wala Mtume. Wala hawana hoja wala ushahidi wa hayo. Na katika haya wanafanana na maneno ya washirikina walio kuwa kabla yao! Mwenyezi Mungu amewalaani makafiri hawa, na atawaangamiza! Ama ajabu watu hawa! Vipi wanaipotea Haki nayo ni dhaahiri inaonekana, na wanakwenda kufuata upotovu. (*Tazama Maelezo 9:30*)

31 Hao Mayahudi na Wakristo wamewafanya makuhani wao na mapadri kuwa ni "Marabi", kama ni miungu, kwa kuwapa madaraka ya kutunga sharia, na kuwa maneno yao ndiyo dini, ijapo kuwa yanakhitalifiana na kauli za Mtume wao. Wanawafuata katika upotovu wao, na wakamuabudu Masihi mwana wa Maryamu! Na Mwenyezi Mungu amewaamrisha katika hivyo hivyo Vitabu vyao kwa ndimi za Mitume wao, kuwa wasimuabudu ila Mungu Mmoja, kwa kuwa Yeye hapana anaye stahiki kuabudiwa kwa mujibu wa hukumu ya sharia na akili ila Mungu Mmoja. Mwenyezi Mungu ametakasika na kushirikishwa katika ibada, umbaji, na sifa.

32 Makafiri wanataka kwa madai yao ya upotovu waizime Nuru ya Mwenyezi Mungu, nayo ni Uislamu. Na Mwenyezi Mungu hataki ila aitimize Nuru yake, kwa kuidhihirisha Dini yake na ashinde Mtume wake, ijapo kuwa wao watachukia.

33 Yeye ndiye Mwenyezi Mungu aliye dhamini kutimiza Nuru yake kwa kumtuma Mtume wake, Muhammad s.a.w. na hoja zilizo wazi, na Dini ya Haki, Uislamu, ipate kutukuka Dini hii juu ya dini zote zilizo tangulia, ijapo kuwa washirikina watakasirika. Mwenyezi Mungu ataipa ushindi tu, wakitaka wasitake.

34 Enyi Waumini! Jueni kuwa wengi katika wataalamu wa Kiyahudi na mapadri wa Kikristo wanajihalalisha kula mali ya watu bila ya haki yoyote, na wanawazuga wafwasi wao wanao waamini kwa kila walisemalo. Na wanawazuilia watu wasiingie katika Uislamu. Na wale wanao kusanya mali, dhahabu na fedha, wakiyaweka tu, wala hawatoi Zaka zake, waonye ewe Mtume, kuwa kuna adhabu ya kutia uchungu --

vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao, wakaambiwa: Haya ndiyo mlio jilimbikia nafsi zenu, basi onjeni mliyo kuwa mkilimbika.³⁵

36. Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na mbili katika hukumu ya Mwenyezi Mungu tangu alipo umbaa mbingu na ardhi. Katika hiyo iko mine mitakatifu. Hiyo ndiyo Dini iliyo sawa. Basi msidhulumu nafsi zenu humo. Na piganeni na washirikina wote kama wao wnavyo pigana nanyi nyote. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu yu pamoja na wachamngu.³⁶

37. Bila ya shaka kuakhirisha (miezi) ni kuzidi katika kukufuru; kwa hayo hupotezwa walio kufuru. Wanauhalalisha mwaka mmoja na kuharimisha mwaka mwingine, ili wafanye kuwa sawa idadi ya ile (miezi) aliyo itukuza Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo huhalalisha alivyo viharimisha Mwenyezi Mungu. Wamepambiwa ubaya wa vitendo vyao hivi. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri.³⁷

38. Enyi mlio amini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache.³⁸

39. Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.³⁹

40. Ikiwa nyinyi hamtamnusuru Mtume, basi Mwenyezi Mungu alikwisha mnusuru walipo mtoa walio kufuru, naye ni wa pili katika wawili walipo kuwa katika pango, naye akamwambia sahibu yake: Usihuzunike. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi. Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamuunga mkono kwa

35 -- Siku ya Kiyama, kwa kuwa hayo mali yatatiwa kwenye Moto wa Jahannamu, kisha waunguzwe nayo kwenye vipaji vya nyuso zao, na mbavu zao, na migongo yao; na waambiwa: Haya ndiyo mliyo kuwa mkijilimbikia kama khazina kwa ajili ya nafsi zenu, wala hamkuwa mkitoa haki ya Mwenyezi Mungu! Basi ionjeni hii leo adhabu kali.

36 Hakika hisabu ya miezi ya kuandama ni miezi kumi na mbili, kwa hukumu na kudra ya Mwenyezi Mungu, na ndivyo alivyo ibainisha katika vitabu vyake tangu kuanza ulimwengu. Na katika hii miezi thinaashara ipo mine imekatzawa kupigana vita ndani yake, nayo: -Mwezi wa Rajab, Alqa'ada (Mfungo Pili), Alhijja (Mfungo Tatu), na Almuhammad (Mfungo Nne). Na huku kuitukuza miezi hii mine na kuharimisha kupigana vita ndani yake ndiyo Dini ya Mwenyezi Mungu Iliyo Nyooka, ambayo haibadiliki wala haina mageuzo. Basi msjidhulumu nafsi zenu kwa kuhalalisha vita katika miezi hii, au mkaacha kujilinda adui akikupigeni. Na enyi Waumini! Piganeni na washirikina bila ya kumbagua yeyote kati yao, kama wanavyo kupigeni nyinyi nyote. Na kuweni na yakini kuwa Mwenyezi Mungu atawanusuru wanao mcha, na wakashika amri zake, na wakaepuka anayo yakataza.

37 Na hakukuwa kuichelewesha miezi mitakatifu, au baadhi yake, kuliko alivyo iweka Mwenyezi Mungu, ila ni kuzidi ukafiri, kama walivyo kuwa wakifanya watu wa kijahiliya. Hao makafiri wakizidisha hivyo kuongeza upotovu juu ya upotovu! Waarabu wakati wa ujahili walikuwa hufanya mwezi uliyo harimishwa kupigana vita kuwa ni wa halali, pindi wakihitajia kupigana. Na hufanya mwezi ulio halalishwa ndio ulio harimishwa. Na wakisema: Mwezi kwa mwezi. Yaani kulipizia ipate kutimia idadi ile aliyo harimisha Mwenyezi Mungu. Matamania yao yamewapendezeshea kitendo chao hicho kiovu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu walio shikilia kukataa kuifuata Njia ya kwenda Kheri.

38 Enyi Waumini! Mna nini, anapo kwambieni Mtume: Tokeni mwende kwenye Jihadi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu baadhi yenu mkafanya uzito kutoka? Haikufalieni hivyo! Mnaona afadhali maisha ya dunia yatayo kwisha, kuliko maisha ya Akhera na neema zake za kudumu? Starehe ya duniani na utamu wake ukilinganisha na starehe ya Akhera ni chache na upuuzi.

39 Msipo muitikia Mtume, mkatoka nje kwenda pigana Jihadi, Mwenyezi Mungu atakupeni adhabu iliyo chungu, na Mola wenu Mlezi atawabadilisha watu waje wengine, sio nyinyi, wamuitikie Mtume wala hawatobaki nyuma ikinadiwa Jihadi. Wala nyinyi kwa kukataa kwenu kwenda pigana, hamtamdhuru Mwenyezi Mungu chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo mkubwa juu ya kila kitu.

majeshi msiyo yaona, na akalifanya neno la walio kufuru kuwa chini, na Neno la Mwenyezi Mungu kuwa ndilo juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu Mwenye hikima.⁴⁰

41. Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito, na piganeni Jihadi kwa mali yenu na nafsi zenu katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Haya ni kheri kwenu mkiwa mnajua.⁴¹

42. Na lau ingeli kuwa ipo faida ya papo kwa papo, na safari yenyewe ni fupi, wangeli kufuata. Lakini wameona ni mbali na kuna mashaka. Nao wataapa kwa Mwenyezi Mungu: Tungeli weza bila ya shaka tungeli toka pamoja nanyi. Wanaziangamiza nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu anajua kuwa hakika hao ni waongo.⁴²

43. Mwenyezi Mungu amekusamehe! Kwa nini ukawapa ruhusa kabla ya kubainikia kwako wanao sema kweli, na ukawajua waongo?⁴³

44. Hawatakuomba ruhusa wale wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, wasende kupigana Jihadi kwa mali yao na nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwajua wachamngu.⁴⁴

45. Wasio muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na nyoyo zao zikatia shaka, hao tu ndio wanao kutaka ruhusa. Basi hao wanataradadi katika shaka zao.⁴⁵

46. Na ingeli kuwa kweli walitaka kutoka bila ya shaka wangeli jilandalia maandalio, lakini Mwenyezi Mungu kachukia kutoka kwao, na kwa hivyo akawazuia na ikasemwa:

40 Enyi Waumini! Ikiwa nyinyi hamtasaidia kumnusuru Mtume wa Mwenyezi Mungu, basi. Kwani Mwenyezi Mungu anatosha Yeye kumnusuru. Kama pale alipo msaidia na akamnusuru alipo tolewa Makka kwa kahari na makafiri, naye hana mwenziwe ila Abu Bakar peke yake. Wakawa wao wawili pangoni wanajificha wasionekane na washirikina walio kuwa wanawasaka wawaadhibu na kuwauwa. Abu Bakar akawa anamkhofia Mtume maisha yake. Mtume akamwambia kumpoza: Usihuzunike! Kwani hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi, kwa kutunusuru na kutusaidia. Hapo Mwenyezi Mungu akamteremshia Abu Bakar utulivu, na akamuunga mkono Mtume kwa askari walio toka kwake, na ambao hawawajui ila Yeye *Subhanahu*. Na mambo yakamalizikia kuwa shari ya washirikina ikavia na Dini ya Mwenyezi Mungu ikashinda. Na Mwenyezi Mungu anasifika kuwa ni Mwenye nguvu, hashindiki, ni Mwenye hikima hapotei katika mipango yake. (*Tazama Maelezo 9:40*)

41 Enyi Waumini! Akinadi mwenye kunadi kuwa kuna Jihadi, basi itikieni wito huo, mkiwa mmoja mmoja au kwa makundi. Kila mmoja kwa kadri ya uwezo wake, na hali mna uchangamfu kwa nguvu na salama na silaha. Na muwanie Jihadi kwa mali na nafsi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kulitukuza Neno la Mwenyezi Mungu. Katika hayo upo utukufu na kheri kwenu, ikiwa nyinyi ni watu wenye ujuzi ulio baraabara na mnajua Haki. (*Tazama Maelezo 9:41*)

42 Qur'ani inawasusuika wanaafiki kwa kubakia nyuma wakaacha kumfuata Mtume katika Jihadi. Ikasema: Ingeli kuwa walicho itiwa hawa wanaafiki ni pato la kidunia lililo jepesi kulipata, au ingeli kuwa safari yenyewe ya kwenda ni nyepesi, wangeli kufuata, ewe Mtume. Lakini wanaona safari hii ina mashaka! Na watakuapia kwamba lau wangeli weza wangeli toka nawe! Na kwa unaafiki huu na uwongo wanajihilikisha nafsi zao. Na hali haimfichikii Mwenyezi Mungu. Yeye anaujua uwongo wao na atawalipa malipo yake.

43 Mwenyezi Mungu amekusamehe, ewe Mtume, kwa kuwaruhusu hawa wanaafiki wabaki nyuma wasende kwenye Jihadi kabla ya kuwa haijabainika kwako ukajua kwamba udhuru wao ni wa kweli, na kuwajua walio waongo kati yao katika madai yao kuwa wanaamini, na kuwa ati wana udhuru za kweli.

44 Sio mwendo wa Waumini wa kweli wanao muamini Mwenyezi Mungu na Hisabu ya Siku ya Mwisho waje kukutaka ruhusa ya kuto kwenda kuwania Jihadi kwa mali na nafsi, au kuwa wao wabaki nyuma wakuache wewe. Kwa sababu ukweli wa Imani yao unawapendekezesha Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anajua ukweli wa niya za Waumini.

45 Wanao kutaka ruhusa ni wale wasio muamini Mwenyezi Mungu kwa Imani ya kweli, wala hawaamini Hisabu yake ya Siku ya Mwisho. Kwa sababu nyoyo zao daima zimo katika shaka na wasiwasi. Nao wanaishi katika hali ya ubabaishi. Na watakuja yapata malipo ya hayo.

Kaeni pamoja na wanao kaa!⁴⁶

47. Lau wangeliki toka nanyi wasingeli kuzidishieni ila mchafuko, na wange tanga tanga kati yenu kukutilieni fitna. Na miongoni mwenu wapo wanao wasikiliza. Na Mwenyezi Mungu anawajua madhaalimu.⁴⁷

48. Tangu zamani walitaka kukutilieni fitna, na wakakupindulia mambo juu chini, mpaka ikaja Haki na ikadhahirika amri ya Mwenyezi Mungu, na wao wamechukia.⁴⁸

49. Na miongoni mwao wapo wanao sema: Niruhusu wala usinitie katika fitina. Kwa yakini wao hivyo wamekwisha tumbukia katika fitina. Na hakika Jahannamu imewazunguka.⁴⁹

50. Ukikupata wema unawachukiza, na ukikusibu msiba, wao husema: Sisi tuliangalia mambo yetu vizuri tangu kwanza. Na hugeuka kwenda zao nao wamefurahi.⁵⁰

51. Sema: Halitusibu ila alilo tuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mola wetu Mlinzi. Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu!⁵¹

52. Sema: Hivyo mnatutazamia litupate lolote isipo kuwa moja katika mema mawili? Na sisi tunakutazamieni kuwa Mwenyezi Mungu akufikishieni adhabu itokayo kwake, au kutokana na mikono yetu. Basi ngojeni, nasi tunangoja pamoja nanyi.⁵²

53. Sema: Toeni mkipenda msipende. Hakitopokelewa kitu kwenu, kwani nyinyi ni watu wapotovu.⁵³

46 Na kama kweli hawa wanaafiki walikuwa na niya ya kwenda kwenye Jihadi pamoja na Mtume, wangeliki jitayarisha kwa vita na wakajiandalia. Lakini Mwenyezi Mungu Mwenyewe alichukia huko kutoka kwao, kwa kuwa akijua lau wangeliki toka nanyi basi wangeliki kuwa dhidi yenu si wenzenu. Basi akawatia uzito wasitoke kwa vile nyoyo zao zilivyo jaa unaafiki! Na msemaji wak akasema: Kaeni pamoja na wale wanao kaa wenye udhuru!

47 Na pindi wangeliki toka pamoja nanyi wasinge kuzidishieni nguvu zozote. Lakini wao wangeeneza wasiwasi na kuzidisha fitna, na wakaieneza kati yenu. Na miongoni mwenu wapo wasio jua uovu wa niya zao, na huenda pengine wangeliki khadaika na maneno yao, na wakazisikiliza fitna zao. Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema hao wanaafiki, wanao jidhulumu nafsi zao kwa ule uharibifu wanao udhamiria.

48 Na hawa wanaafiki walikwisha tangulia kuleta fitna baina yenu, na wewe, ewe Mtume, wakakupangia njama. Lakini Mwenyezi Mungu aliviviza vitimbi vyao, na akahakikisha kukunusuru, na akaipa ushindi Dini yake wao wakipenda wasipende.

49 Na baadhi ya wanaafiki walikuwa wakimwambia Mtume: Tupe ruhusa tukae tusende kwenye Jihadi, wala usitutie kwenye shida na dhiki. Na wao kwa hakika kwa msimamo huo wamekwisha jitia wenyewe katika maasia, kumuasi Mwenyezi Mungu. Na hakika Siku ya Akhera Moto wa Jahannamu utawazunguka.

50 Hawa wanaafiki hawakutakii wewe Mtume na Masahaba zako ila mambo ya karaha tu. Wanaona uchungu mkipata kheri yoyote, ikiwa ya ushindi au ngawira; na wanafurahi mkisibiwa na shari, kama kujeruhiwa au kuuwawa! Na yakikupateni hayo wao husema kwa kufurahia msiba wenu: Sisi tulichukua hadhari yetu, kwa kubaki nyuma tusitoke kwenda kwenye Jihadi. Na huenda zao nao wamefurahi.

51 Waambie ewe Mtume: Hayatupati ya kheri wala ya shari katika hii dunia yetu, ila aliyo tukadiria Mwenyezi Mungu. Kwani sisi turadhi na hukumu ya Mwenyezi Mungu. Hatujitapi kwa kheri, wala hatuingiwi na dukuduku la roho kwa kufikiwa na shari. Hakika Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kuyatawala mambo yetu yote, na juu yake Yeye tu ndio Waumini wa kweli wanategemea.

52 Ewe Mtume! Waambie hao: Nyinyi msitaraji yatatufikia sisi ila moja ya mema mawili, ama tushinde na tupate ngawira, au tufe mashahidi katika Njia ya Mwenyezi Mungu na tuingie Peponi kesho Akhera. Na sisi tunakutarajieni ikufikieni adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu ikuangamizeni; au akuadhibuni kwa udhalili kutokana na mikono yetu. Basi ingojeeni amri ya Mwenyezi Mungu; na sisi pia tunaingoja amri yake pamoja nanyi.

53 Ewe Mtume! Waambie hao wanaafiki wanao taka kuficha unaafiki wao kwa kutoa michango ya mali kwa ajili ya Jihadi na mengineyo: Toeni mtakacho, kwa khiari au kwa nguvu; Mwenyezi Mungu havikubali vitendo vyenu vilivyo kwisha haribiwa na unaafiki wenu! Kwani nyinyi daima ni wenye kuiasi Dini ya Mwenyezi Mungu, wenye kuipinga amri yake.

- 54.** Na hawakuzuliwa kukubaliwa michango yao ila kwa kuwa walimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala hawaji kwenye Sala ila kwa uvivu, wala hawatoi michango ila nao wamechukia.⁵⁴
- 55.** Yasikufurahishe mali yao wala wana wao. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaadhibu kwayo hapa duniani, na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri.⁵⁵
- 56.** Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba wao ni katika nyinyi, wala wao si katika nyinyi. Lakini ni watu wanao ogopa.⁵⁶
- 57.** Lau kama wangeli pata pa kukimbilia au mapango au pahala pa kuingia basi wangeli fyatuka mbio kuelekea huko.⁵⁷
- 58.** Na miongoni mwao wapo wanao kusengeny katika kugawa sadaka. Wanapo pewa wao huridhika. Na wakito pewa hukasirika.⁵⁸
- 59.** Na laiti wao wangeli ridhia kile alichu wapa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakasema: Mwenyezi Mungu anatosheleza, Mwenyezi Mungu atatupa katika fadhila yake - na pia Mtume wake; hakika sisi ni wenye kumtaka Mwenyezi Mungu!⁵⁹
- 60.** Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanao zitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni waajibu ulio faridhiwa na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.⁶⁰

54 Wala Mwenyezi Mungu hakukataza visipokelewe wanavyo vitoa ila kwa kuwa wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na ukafiri, kukataa, kunavunja a'mali zote. Na vile kwa kuwa wao hawasali kwa namna walio amrisha; kwani wao husali bila ya kuiamini Sala, ila wanafanya kama ni kuficha unaafiki wao. Wala wao hawatoi kitu isipo kuwa na huku wanachukia huko kutoa ndani ya nyoyo zao.

55 Wala usifurahie na moyo wako ukavutika kwa unavyo waona wanaafiki wana mali na wana. Kwani Mwenyezi Mungu hakuwapa hayo ila wapate kuyahangaikia hayo kwa taabu na mashaka wayalinde katika maisha ya duniani, bila ya kupata malipwa yake. Yawakumbe mauti nao wamo katika ukafiri wao, waadhibiwe kwa sababu yake Akhera.

56 Na hawa wanaafiki hukuapieni kiapo cha uwongo, enyi jamaa Waumini, kwamba wao ni Waumini kama nyinyi. Na hakika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu. Lakini hao ni watu madhaifu na woga, na hayo ndiyo yanayo wapelekea kufanya unaafiki wao, na daima kuwa na khofu.

57 Wao hali wanakudhikini na wanachukia kuingiana nanyi, lau wangeli pata ngome, au mapango milimani, au mashimo chini ya ardhii wakaingia humo, basi wangeli yakimbilia mbio!

58 Na baadhi ya hawa wanaafiki wanakusema kwa ubaya, na wanakutia ila katika ugawaji wa sadaka na ngawira. Hawana ila uroho wa makombo ya kidunia tu. Ukiwapa wakitakacho wanakuwa radhi nawe kwa utendayo. Na kama hukuwapa ndio wao ni wepesi wa kukuletea maudhi.

59 Na lau kuwa hao wanaafiki wanao kusema kwa vibaya katika ugawaji wa sadaka na ngawira wangeli ridhia wanacho gaiwa na Mwenyezi Mungu, nacho ndicho anacho wapa Mtume wake, na zikatua nafsi zao - ijapo kuwa ni kitu kidogo - na wakasema: Hukumu ya Mwenyezi Mungu imetutosheleza, na Mwenyezi Mungu ataturuzuku kutokana na fadhila yake, na Mtume wake atakuja tupa zaidi kuliko alichu tupa mara hii, na sisi tunataka ut'iifu wa Mwenyezi Mungu na fadhila zake na ihsani zake.. lau wangeli fanya hayo ingeli kuwa kheri kwao.

60 Zaka iliyo faridhiwa haitumiwi ila kwa mafakiri wasio pata cha kuwatosha, na masikini wagonjwa ambao hawawezi kazi wala hawana mali, na wale wanao itumikia kwa kuikusanya, na wanao tiwa moyo kwa sababu wanatarajiwa kusilimu na kupatikana kwao manufaa kwa utumishi wao na kuunusuru Uislamu, na wale wanao eneza Uislamu na kufanya tabshiri (Da'awa), na katika kuwakomboa waliomo utumwani na walio tekwa, na kuwatoa waliomo katika unyonge na utawala wa madhila, na katika kuwalipia wenye madeni walio shindwa kuyalipa ikiwa hayo madeni hayakutokana na madhambi au dhulma au upumbavu, na katika kuzatiti Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na katika mambo kama hayo yaliyomo katika njia za kheri na wema, na katika kusaidia wasafiri walio katikiwa kupata msaada wa mali yao na watu wao. Mwenyezi Mungu ameyatungia sharia hayo kuwa ni waajibu kwa ajili ya maslaha ya waja wake. Na

61. Na miongoni mwao wapo wanao muudhi Nabii na kusema: Yeye huyu ni sikio tu. Sema: Basi ni sikio la kheri kwenu. Anamuamini Mwenyezi Mungu, na ana imani na Waumini, naye ni rehema kwa wanao amini miongoni mwenu. Na wanao muudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu watapata adhabu chungu.⁶¹
62. Wanakuapieni Mwenyezi Mungu ili kukuridhisheni nyinyi, hali ya kuwa wanao stahiki zaidi kuridhishwa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake, lau kama wao ni Waumini.⁶²
63. Je, hawajui ya kwamba anaye shindana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi huyo atapata Moto wa Jahannamu adumu humo? Hiyo ndiyo hizaya kubwa.⁶³
64. Wanaafiki wanaogopa isije teremshwa Sura itakayo watajia yaliyomo katika nyoyo zao. Sema: Fanyeni mzaha! Hakika Mwenyezi Mungu atayatoa nje hayo mnayo yaogopa.⁶⁴
65. Na ukiwauliza, wanasema: Sisi tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu. Sema: Mlikuwa mkimfanyia maskhara Mwenyezi Mungu na Ishara zake na Mtume wake?⁶⁵
66. Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu! Tukilisamehe kundi moja kati yenu, tutaliadhibu kundi jingine kwa kuwa wao ni wakosefu.⁶⁶
67. Wanaume wanaafiki na wanawake wanaafiki, wote ni hali moja. Huamrisha maovu na huyakataza mema, na huifumba mikono yao. Wamemsahau Mwenyezi Mungu, basi na Yeye pia amewasahau. Hakika wanaafiki ndio wapotofu.⁶⁷

Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni Mwenye kujua vyema maslaha ya viumbe vyake, na Mwenye hikima kwa anayo yafanyia sharia. (*Tazama Maelezo 9:60*)

61 Na wapo watu wanaafiki wanakusudia kumuudhi Nabii, na kumlelea ya kumkirih. Wao humtuhumu kuwa anapenda kusikiliza kila analo ambiwa, kweli na uwongo, na kwamba yeye anakhadaika na hayo anayo yasikia. Basi, ewe Mtume! Waambie: Huyo mnaye msengenya nyuma yake sio kama mnavyo dai. Bali yeye ni sikio la kheri kwenu. Hasikii ila la kweli, wala hakhadaiki na upotovu. Anamsadiki Mwenyezi Mungu na wahyi (ufunuo) wake, na anawasadiki Waumini, kwa sababu Imani yao inawakataza uwongo. Na yeye ni rehema kwa kila mmoja wenu anaye amini. Na hakika Mwenyezi Mungu amewaandalia wanao muudhi Mtume adhabu chungu, na kali, na ya kudumu milele.

62 Katika kwenda vitani wao hubaki nyuma hawatoki nanyi kwenda kupigana na adui zenu wala hawataradadi. Na kisha hukutoleeni udhuru wa uwongo kwa kule kubaki kwao nyuma. Na hukuapieni ili muwaridhie na mkubali udhuru wao. Na wa kustahiki kutakiwa radhi kama wao kweli ni Waumini, ni Mwenyezi Mungu na Mtume.

63 Hivyo hawa wanaafiki hawajui kwamba malipo ya mwenye kumkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na akashindana nao ni adhabu ya daima katika Moto wa Jahannamu? Na hiyo ndiyo hizaya ya kufedhehesha, na madhila makubwa.

64 Wanaafiki wanapo kuwa wao kwa wao humfanyia kejeli Mtume, na wao wanaogopa yasifedheheke mambo yao, zikamteremkia Nabii Aya za Qur'ani zitakazo fichua yale wanayo yaficha katika nyoyo zao, na wanayafanya ni siri baina yao! Ewe Mtume! Waambie: Fanyeni maskhara yenu mpendavyo, Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyafichua hayo mnayo yaogopea yasije kudhihiri

65 Ewe Mtume! Kuwa na yakini kwamba, baada ya kwisha fedheheka mambo yao hawa wanaafiki, ukawauliza sababu ya kuitia ila Dini na kumfanyia kejeli Mwenyezi Mungu na Ishara zake, wao hutoa udhuru kwa kusema: Tulikuwa tunapiga porojo na tukicheza tu! Waambie: Vipi inakufalieni kupiga porojo na kucheza kwa kumfanyia maskhara Mwenyezi Mungu na Aya zake na Mtume wake?

66 Msitoe udhuru kama huu wa uwongo! Ukafiri wenu umekwisha dhiri baada ya kujidai kwenu kuwa mmeamini. Na ikiwa Sisi tutalisamehe kundi moja lenu lilio tubu na likaamini, kwa sababu ya kutubu kwake kwa kweli, na kuamini kwake, vile vile tutaliadhibu kundi jingine katika nyinyi kwa kushikilia kwake ukafiri na unaafiki, na ukhalifu wake katika haki ya Mtume na ya Waumini

67 Wanaafiki wanaume na wanaafiki wanawake wamefanana kwa kuwa wote wanatenda maovu, na wanayaamrisha, na wanaiacha Haki na wanaikataza, na wanafanya ubakhili kutumia mali katika njia za kheri. Basi hao kama ni viungo vya mwili mmoja. Wamemwacha Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi

68. Mwenyezi Mungu amewaahidi wanaafiki wanaume na wanaafiki wanawake na makafiri Moto wa Jahannamu kudumu humo. Hayo yanawatoshia, na Mwenyezi Mungu amewalaani; nao wana adhabu milele.⁶⁸

69. Ni kama wale walio kuwa kabla yenu. Walikuwa wana nguvu na mali na watoto zaidi kuliko nyinyi. Basi walistarehea fungu lao, na nyinyi mnastarehea fungu lenu, kama walivyo starehe kwa fungu lao wale walio kuwa kabla yenu. Na nyinyi mkazama katika maovu kama wao walivyo zama. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika katika dunia na Akhera; na hao ndio walio khasiri.⁶⁹

70. Je, hazikuwafikia khabari za walio kuwa kabla yao - kaumu ya Nuhu, na A'ad, na Thamud, na kaumu ya Ibrahim, na watu wa Madyana, na miji iliyo pinduliwa chini juu? Mitume wao waliwafikia kwa hoja zilizo wazi. Basi Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuwadhulumu, walakini wao walikuwa wakijidhulumu wenyewe.⁷⁰

71. Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hikima.⁷¹

72. Mwenyezi Mungu amewaahidi Waumini wanaume na Waumini wanawake Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na makaazi mema katika Bustani za kudumu, na Radhi za Mwenyezi Mungu ndio kubwa kuliko yote. Huko ndiko kufuzu kukubwa.⁷²

Mungu naye akawaacha wala hawaongoi, kwa kuwa wao wamekwisha toka kwenye ut'iifu wa Mwenyezi Mungu.

68 Mwenyezi Mungu amewaandikia wanaafiki na makafiri Moto wa Jahannamu. Atawaadhibu humo, wala hawatatoka. Hayo yanatosha kuwa ni malipo yao, na pamoja na malipo hayo watapata kukasirikiwa na Mwenyezi Mungu na adhabu ya daima Siku ya Kiyama.

69 Hakika hali yenu, enyi wanaafiki, ni kama hali ya wenzenu walio kutangulieni katika unaafiki na ukafiri. Kwa hakika wao walikuwa wana nguvu zaidi kuliko nyinyi, na walikuwa na mali zaidi na watoto. Wakajistarehea kwa sehemu yao ya dunia walio jaaliwa, na wakapuza kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kumcha Yeye. Na wakawakabili Manabii wao kwa kuwabeua na kuwakejeli. Na nyinyi mmejistarehea vile vile kwa mlivyo jaaliwa katika ladha za kidunia, kama walivyo jistarehea wao. Na nyinyi mkabobea katika mambo machafu na mapotovu kama walivyo bobea wao. Hakika hao vitendo vyao vimeharibika, basi havikuwafaa duniani wala Akhera, na wakawa wenye kukhasiri. Na nyinyi ni mfano wa hao katika hali na matokeo maovu.

70 Basi je, hawazingatii wanaafiki na makafiri hali ya walio watangulia katika kaumu ya Nuhu na A'ad na Thamud na kaumu ya Ibrahim na kaumu ya Shuaib na kaumu Lut'? Mitume wa Mwenyezi Mungu waliwajia na hoja zilizo wazi wazi kutokana na Mwenyezi Mungu, na wakawakanusha na wakawakataa! Mwenyezi Mungu akawashika kila mmoja wao kwa dhambi zake, na akawateketeza wote! Wala Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu, lakini walizidhulumu wenyewe nafsi zao kwa ukafiri wao, na uasi wao kumuasi Mwenyezi Mungu, na wakastahiki peke yao kupata adhabu. Basi wao ndio wanao jidhulumu wenyewe.

71 Na Waumini wanaume na Waumini wanawake, wao kwa wao ni wapenzi wa kupendana na kusaidiana, kwa mujibu wa Imani. Wanaamrisha yanayo amrishwa na Dini yao ya Haki, na wanakataza yanayo katazwa na Dini. Wanatimiza Sala kwa nyakati zake, wanatoa Zaka kuwapa wanao stahiki kwa wakati wake. Na wanat'ii anayo waamrisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na wanayaepuka anayo yakataza Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na hao ndio watakao kuwa chini ya Rehema ya Mwenyezi Mungu, kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwalinda kwa Rehema, na Mwenye hikima katika upaji wake.

72 Mwenyezi Mungu amewaahidi hao Bustani (Pepo) watakao kaa daima katika neema zake, na makaazi ya kuziliwaza nafsi zao katika makao ya kudumu milele. Na pamoja na hayo watapata Radhi ya Mwenyezi Mungu kuwa radhi nao, nayo wataiona. Na hiyo ndiyo neema kubwa kabisa. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.

- 73.** Ewe Nabii! Pambana na makafiri na wanaafiki, na wakazanie. Na makaazi yao ni Jahannamu, na huo ndio mwisho mbaya.⁷³
- 74.** Wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hawakusema; nao wamekwisha sema neno la ukafiri, na wakakufuru baada ya kusilimu kwao. Na wakajihimu kufanya ambayo hawakuweza kuyafikia. Na hawakuchukia ila kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake amewatajirisha kutokana na fadhila zake. Wakitubu itakuwa kheri kwao, na wakigeuka Mwenyezi Mungu atawaadhibu adhabu chungu duniani na Akhera. Na wala hawana katika ardhi mlinzi wala wa kuwanusuru.⁷⁴
- 75.** Na miongoni mwao wapo walio muahidi Mwenyezi Mungu kwa kusema: Akitupa katika fadhila yake hapana shaka tutatoa sadaka, na tutakuwa katika watendao mema.⁷⁵
- 76.** Alipo wapa katika fadhila yake wakaifanyia ubakhili na wakageuka, na huku wakipuuzua.⁷⁶
- 77.** Basi akawalipa unaafiki kuutia nyoyoni mwao mpaka Siku watapo kutana naye, kwa sababu ya kuwa walimkhalifu Mwenyezi Mungu katika yale waliyo muahidi, na kwa sababu ya kusema kwao uwongo.⁷⁷
- 78.** Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anajua siri zao na minong'ono yao, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua sana ya ghaibu?⁷⁸
- 79.** Wale wanao wabeuwa Waumini wanao toa sadaka nyingi na wasio nacho cha kutoa ila kadri ya juhudi yao, basi huwakejeli. Mwenyezi Mungu atawakejeli wao! Nao watapata adhabu chungu!⁷⁹
- 80.** Waombe msamaha au usiwaombe. Hata ukiwaombe msamaha mara sabiini, Mwenyezi Mungu hatawasamehe. Hayo ni kwa sababu ya kuwa wao wamemkataa

73 Ewe Nabii! Shikamana na juhudi ya kuwazuia makafiri na ukafiri wao, na wanaafiki na unaafiki wao. Na wakazanie katika juhudi yako. Makaazi yao hawa aliyo waahidi Mwenyezi Mungu huko Akhera ni Jahannamu. Na uovu ulioje mwisho huo!

74 Hao wanaafiki wanaapa mbele yako, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwamba hawakusema jambo baya katika hayo uliyo ambiwa. Nao ni waongo katika kukataa kwao, wanaapa kiapo cha uwongo! Na wao hakika wamesema neno la kufuru. Na ukafiri wao sasa umebainika, baada ya kuwa kwanza umefichika. Na hapana sababu yoyote ya kukuchukia ila ni kiburi kwa neema walizo pewa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kwa kule kupewa ngawira walizo shirikiana na Waislamu! Wakirejea kwa Mwenyezi Mungu, wakaacha unaafiki wao, na wakajuta kwa waliyo yatenda, toba yao itakubaliwa. Na hivyo itakuwa kheri kwao. Wakiitupa Imani, basi Mwenyezi Mungu atawaadhibu duniani kwa namna mbali mbali za balaa, na kesho Akhera atawatia katika Moto wa Jahannamu. Wala hawatapata katika ardhi wa kuwapigania, au wa kuwaombea, au wa kuwanusuru.

75 Katika wanaafiki wapo ambao humuapia na kumuahidi Mwenyezi Mungu kuwa akiwapa mali na akawatajirisha kwa fadhila yake, basi watatoa sadaka na watakuwa wenye vitendo vyema.

76 Mwenyezi Mungu akiwaitikia na akawapa kwa fadhila yake, wanafanya ubakhili. Hawatoi kitu, wala hawatimizi ahadi, na huiacha kheri wakiipuuzua na wakimpuuzua Mwenyezi Mungu.

77 Matokeo ya ubakhili wao ni kujaa unaafiki katika nyoyo zao mpaka watakapo kufa na wakakutana na Mwenyezi Mungu, kwa sababu ya kuvunja ahadi zao na uwongo wao katika viapo vyao.

78 Vipi wanajitia ujinga na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwajua vyema? Hapana chochote wanacho dhamiria kisirisiri katika kuvunja ahadi kinacho fichikana kwake. Wala wanacho kinong'ona kwa uficho katika kuitia kombo Dini na kuwapangia njama Waislamu. Naye, aliye tukuka shani yake, ni Mjuzi mno hapitikiwi na kitu chochote.

79 Na katika ila zao hawa wanaafiki pamoja na ubakhili wao ni kuwa wao huwakejeli Waumini wenye nafasi kwa vile kusabilia mali yao kwa wanao hitajia, na huwafanyia maskhara wale wenye nafasi ndogo wanao toa sadaka juu ya kuwa wenyewe walicho nacho ni kidogo. Mwenyezi Mungu kesha walipa kwa hizo kejeli zao kwa kuwakashifu wakatambulikana fedheha zao, wakawa wao ndio kichekesho cha watu wote. Na kesho Akhera adhabu yao itakuwa kali.

Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotofu.⁸⁰

81. Walifurahi walio achwa nyuma kwa kule kubakia kwao nyuma na kumuacha Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walichukia kupigana Jihadi kwa mali zao na nafsi zao, na wakasema: Msitoke nje katika joto! Sema: Moto wa Jahannamu una joto zaidi, laiti wangedi fahamu!⁸¹

82. Basi nawacheke kidogo; watalia sana. Hayo ni malipo ya yale waliyo kuwa wakiyachuma.⁸²

83. Basi Mwenyezi Mungu akikurudisha kwenye kikundi kimoja miongoni mwao - na wakakutaka idhini ya kutoka - sema: Nyinyi hamtatoka pamoja nami kabisa, wala hamtapigana na adui pamoja nami. Nyinyi mliridhia kukaa nyuma mara ya kwanza, basi kaeni pamoja na hao watakao bakia nyuma.⁸³

84. Wala usimsalie kabisa yeyote katika wao akifa, wala usisimame kaburini kwake. Hakika hao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakafa na hali ni wapotofu.⁸⁴

85. Wala zisikushitue mali zao na watoto wao. Mwenyezi Mungu anataka kuwaadhibu kwa hayo katika dunia; na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri.⁸⁵

86. Na inapo teremshwa Sura isemayo: Muaminini Mwenyezi Mungu na piganeni Jihadi pamoja na Mtume wake, wale wenye nguvu miongoni mwao hukutaka ruhusa

80 Haitofaa kitu kuwaitikia baadhi yao na ukawaombea maghfira kwa Mwenyezi Mungu. Ewe Nabii! Ukiwaombea msamaha au ukitowaombea, hata ukiwaombea mara ngapi, Mwenyezi Mungu hatowasamehe! Kwa sababu kwa hawa hapana matarajio ya msamaha wala maghfira maadamu wanaendelea na ukafiri wao. Na watu hawa wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wanao kwenda kinyume naye, wakamuasi, na wakenda kinyume na kumuasi Mtume wake, na wakaiasi Sharia yake na Dini yake.

81 Hakika wanaafiki walibaki nyuma wasitoke pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenda kuwakaabili maadui, na wakafurahi kubakia Madina baada ya kutoka Nabii, na kukhalifu amri yake ya kwenda kwenye Jihadi. Walichukia kutumia mali yao na kujitolea roho zao kwa ajili ya Jihadi kulinyanyua Neno la Mwenyezi Mungu na kuinusuru Dini yake. Wakawa wao wakiwavunja moyo wengineo, na wakiwashawishi wabaki nyuma pamoja nao, na wakiwatisha wasende vitani katika joto kama hilo! Ewe Mtume! Waambie hawa: Kama nyinyi mna akili mtakumbuka kuwa vukuto la Moto wa Jahannamu ni kali zaidi na lina shida zaidi kuliko hili mnao likhofu.

82 Basi nawacheke kufurahia kutokwenda vitani na kuwakejeli Waumini. Kwani kicheko chao muda wake ni mfupi; kitakwisha yatakapo kwisha maisha yao hapa duniani. Tena kitafuata kilio kikubwa kisicho kuwa na mwisho cha huko Akhera. Hayo ni malipo yao kwa madhambi waliyo yafanya.

83 Ukirejea kutoka vitani wakawa baadhi ya hawa wanaafiki walio kataa kwenda vitani wakakutaka ruhusa watoke nawe kwenda Jihadi katika vita vingine, basi wewe usiwakubalie, na waambie: Hamtokwenda nami katika vita vyo vyote, wala hamtoshirikiana nami katika kupigana kokote na adui. Kwani kukaa kwenu nyuma msitoke pale mara ya kwanza hakukuwa na udhuru wowote unao faa, wala haikutokea toba yoyote ya kustahiki msamaha! Basi kaeni kama mliyoye ridhia kukaa pamoja na wazee na wakongwe na wanawake na watoto wadogo walio bakia nyuma.

84 Na akifa yeyote katika wao, basi usimsalie, wala usisimame kaburini kwake anapo zikwa, kwa sababu hawa wameishi maisha yao nao wakimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wao wamekufa, nao wametoka katika Dini ya Mwenyezi Mungu.

85 Wala usistaajabu, ewe Mtume, kuona tulivyo wapa mali na wana, juu ya kuwa tumeudhika nao. Hayakuwa hayo kwa kuwa tunawapendelea wao zaidi, lakini ni kutekeleza anayo yataka Mwenyezi Mungu yawapate, nayo ni shakawa ya duniani kwa kushughulikia kukusanya mijimali tu pamoja na yaliyo lazimikana nayo. Nayo ni hizo hamu na masaibu yanayo ambatana na ukusanyaji wa mali. Na ili yatimie anayo yataka Mwenyezi Mungu yawe, nayo ni kuwa waifariki dunia nao ni makafiri, iwe wamekhasiri dunia na Akhera.

na husema: Tuache tuwe pamoja na wanao kaa nyuma!⁸⁶

87. Wameridhia kuwa pamoja na wabakiao nyuma, na nyoyo zao zikapigwa muhuri; kwa hivyo hawafahamu.⁸⁷

88. Lakini Mtume na wale walio amini pamoja naye waliwania Jihadi kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio watakao pata kheri nyingi, na hao ndio wenye kufanikiwa.⁸⁸

89. Mwenyezi Mungu amewatengenezea Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Huko ndiko kufuzu kukubwa.⁸⁹

90. Na walikuja wenye kutoa udhuru katika Mabedui ili wapewe ruhusa, na wakakaa wale walio mwambia Mwenyezi Mungu na Mtume wake uwongo. Itawafika walio kufuru katika wao adhabu chungu.⁹⁰

91. Hapana lawama kwa wanyonge, wagonjwa, na wasio pata cha kutumia, maadamu wanamsafia niya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hapana njia ya kuwalaumu wanao fanya wema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.⁹¹

92. Wala wale walio kujia ili uwachukue ukasema: Sina kipando cha kukuchukueni. Tena wakarudi na macho yao yanamiminika machozi kwa huzuni ya kukosa cha kutoa.⁹²

93. IPO NJIA ya kuwalaumu wale wanao kuomba ruhusa wasende vitani na hali wao ni matajiri. Wameridhia kuwa pamoja na wanao bakia nyuma. Na Mwenyezi Mungu amewapiga muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawajui.⁹³

86 Na hawa wanaafiki wakisikia chochote ulicho teremshiwa katika Qur'ani kinacho wataka wamsafie Imani Mwenyezi Mungu, na wende kwenye Jihadi pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu, matajiri na wenye nguvu katika wao wanakutaka uwaachilie wasende nawe kwenye Jihadi, na husema: Tuache tuwe na hawa walio pewa ruhusa kukaa nyuma Madina.

87 Hao hakika wamejikubalia wenyewe wahisabike katika walio bakia nyuma, nao ni wanawake, na wasio jiweza, na watoto wadogo wasio viweza vita. Na Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao kwa khofu na unaafiki. Basi hao hawafahamu vilivyo uhakika wa Jihadi na kumfuata Mtume, nako ni kupata utukufu duniani na kupata radhi ya Mwenyezi Mungu katika Akhera.

88 Hiyo ndiyo hali ya wanaafiki. Lakini Mtume na wale walio sadiki pamoja naye, wametoa mali zao na roho zao ili kumridhi Mwenyezi Mungu, na kulinyanuya Neno lake. Hao tu peke yao ndio watakao pata kila kheri ya duniani, nayo ni utukufu na ushindi, na a'mali njema. Na wao peke yao ndio wenye kufuzu.

89 Na Mwenyezi Mungu amekwisha watengenezea katika Akhera neema za kudumu, katika Mabustani yanayo pitiwa na mito. Na huko ndiko kufuzu adhimu, na kufanikiwa kukubwa.

90 Na kama walivyo bakia nyuma baadhi ya wanaafiki katika Madina wasitoke kwenda pigana Jihadi, kadhaalika walikuja baadhi ya Mabedui, nao ni watu wa majangwani, wakijidai kutoa udhuru huu na huu ili waruhusiwe wabaki nyuma. Na kwa hivyo wakakaa nyuma wale walio mwambia uwongo Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kuonyesha Imani. Hawakuhudhuria, wala hawakumtaka udhuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na hiyo ni dalili ya ukafiri wao. Adhabu ya kutia uchungu itawateremkia walio makafiri kati yao.

91 Hakika wanao kubaliwa udhuru wao kubaki nyuma ni wanyonge, na madhaifu wasio jiweza, na wagonjwa, na mafakiri wasio pata cha kutumia kujizatiti kwa vita. Na watu hawa wakiwa wao wana usafi wa niya kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika Dini yao, basi hao ni watu wema, wala hapana lawama juu ya watu wema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira, na Mkunjufu wa Rehema.

92 Na kadhaalika hapana lawama juu ya Waumini wanao kujia uwapatie kipando cha kwendea Jihadi ukawaambia: Sina cha kukupandisheni. Wakenda zao na macho yao yanatiririka machozi kwa huzuni ya kukosa sharafu ya Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, kwa kukosa kwao masurufu ya kutoa.

93 Lawama na adhabu ni juu ya wale wanao kutaka ruhusa, ewe Mtume, wabakie nyuma wasende vitani, nao wanayo mali na zana, na wanaweza kutoka pamoja nawe. Kwani hao juu ya uwezo wao wamekhiari wabaki nyuma pamoja na wanawake wanyonge, na wazee wakongwe, na wagonjwa wasio jiweza; na nyoyo zao hao zimefungwa hazitambui Haki, na hawajui matokeo maovu kabisa yatakayotokea duniani na Akhera kwa kule kuacha kutoka kwao kwenda kwenye Jihadi.

94. Watakutoleeni udhuru mtapo warudia. Sema: Msitoe udhuru; hatukuaminini. Mwenyezi Mungu amekwisha tueleza khabari zenu. Na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wataviona vitendo vyenu. Kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa ya siri na ya dhaahiri; naye atakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.⁹⁴
95. Watakuapieni kwa Mwenyezi Mungu mtakapo rudi kwao ili muwaachilie mbali. Basi waachilien mbali. Hakika hao ni najsi, na makaazi yao ni Jahannamu, kuwa ni malipo kwa waliyo kuwa wakiyachuma.⁹⁵
96. Wanakuapieni ili muwe radhi nao. Basi hata mkiwa radhi nao nyiye, Mwenyezi Mungu hawi radhi na watu wapotofu.⁹⁶
97. Mabedui wamezidi sana katika ukafiri na unaafiki, na wameelekea zaidi kutojua mipaka ya aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.⁹⁷
98. Na katika Mabedui hao wapo wanao fikiri kuwa wanayo yatoa ni gharama ya bure, na wanakungojeleeni mambo yakugeukieni. Mageuko maovu yatakuwa juu yao! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.⁹⁸
99. Na katika Mabedui wapo wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wanaitakidi kuwa wanayo yatoa ndiyo ya kuwasogeza kwa Mwenyezi Mungu na ya kuwapatia dua za Mtume. Naam! Hayo ni kweli mambo ya kuwasogeza. Mwenyezi Mungu atawaingiza katika rehema yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira Mwenye kurehemu.⁹⁹

94 Enyi Waumini Mujaahidina! Hao walio bakia nyuma na wakafanya taksiri watakutoleeni udhuru mtapo rejea kutoka vitani na mkakutana nao. Ewe Mtume! Waambie: Msitoe udhuru, kwani hakika sisi hatukusadikini. Mwenyezi Mungu amekwisha bainisha wazi ukweli wa roho zenu, na amemfunulia Nabii wake baadhi ya uwongo wenu. Na baada ya hayo Mwenyezi Mungu na Mtume wake watavijua vitendo vyenu. Na mwisho wenu baada ya maisha ya duniani ni kuendea kwa Mwenyezi Mungu ambaye anayajua yaliyo fichikana na yanayo onekana wazi. Naye atakulipeni kwa mliyo kuwa mkiyatenda. Na atakulipeni kwa mnavyo stahiki.

95 Watakuapieni kwa Mwenyezi Mungu pale mtapo rejea kwao, kwamba wao wanasema kweli katika kutoa udhuru wao, ili muwaridhie na kwa hivyo waghafilike na vitendo vyao. Basi msiwakubalie kwa lengo lao hilo. Bali watengeni na muwachukie, kwani wao wako daraja ya mwisho kabisa ya ukhabithi wa roho na ukafiri. Na mwisho wao ni Jahannamu, kuwa ndio adabu yao kwa madhambi na maasi walio yatenda!

96 Wanakuapieni kwa tamaa ya kutaka muwe radhi nao. Hata mkakhadaika kwa viapo vyao na mkawaridhia, radhi zenu nyinyi peke yenu hazitowafaa, kwa sababu Mwenyezi Mungu amekasirika nao kwa upotovu wao na uasi wao kuipinga Dini.

97 Mabedui, Waarabu wa majangwani, ndio wakubwa wa kuikataa Haki na wa unaafiki. Hao hakika wamefika upeo wa mwisho katika hayo. Na hayo ni hivyo kwa kuwa wao wapo mbali na maarifa na mwahali mwenye vitovu vya ilimu. Na wao ndio wameelekea zaidi kuwa wasijue mipaka ya Mwenyezi Mungu, na aliyo mteremshia Mtume wake katika sharia na hukumu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa pande zote mbili, na ni Mwenye hikima katika malipo anayo yakadiria.

98 Na baadhi ya hawa wanaafiki katika watu wa majangwani wanaona kuwa wanacho kitoa katika *Sabiili-Llahi* (Njia ya Mwenyezi Mungu) kuwa ni gharama na khasara ya bure, kwa kuwa vile hawaamini kuwa kuna malipo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nao wanataraji na wanangojewa hali ya vita ikugeukieni nyinyi Waumini. Bali hayo mageuko yatawageukia wao! Na hiyo shari wanayo ingojea ikufikieni itawafika wao iwazunguke! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuzisikia kauli zao, na Mwenye kuvijua vitendo vyao na niya zao, na madhambi wanayo yachuma.

99 Wala si kama Mabedui wote ni hali hiyo. Wamo kati yao wanao muamini Mwenyezi Mungu, na wanaisadiki Siku ya Kiyama, na wanaitakidi kuwa kwa kutoa katika Njia ya Mwenyezi Mungu wanajikaribisha kwa Mwenyezi Mungu, na ni sababu ya Mtume s.a.w. kuwaombea wao, kwa kuwa yeye alikuwa akiwaombea kheri na baraka wale wanao toa sadaka. Na hayo bila ya shaka ni njia kubwa ya

100. Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.¹⁰⁰

101. Na katika mabedui walio jirani zenu wamo wanaafiki; na katika wenyeji wa Madina pia wapo walio bobea katika unaafiki. Wewe huwajui. Sisi tunawajua. Tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa.¹⁰¹

102. Na wengine walikiri dhambi zao, wakachanganya vitendo vyema na vingine viovu. Asaa Mwenyezi Mungu akapokea toba zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.¹⁰²

103. Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombe rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.¹⁰³

104. Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja wake, na anazikubali sadaka, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kupokea toba na Mwenye kurehemu?¹⁰⁴

105. Na sema: Tendeni vitendo. Na Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Waumini wataviona vitendo vyenu. Na mtarudishwa kwa Mwenye kujua siri na dhaahiri; naye atakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.¹⁰⁵

kuwakaribisha watu kwa Mwenyezi Mungu na kuwafikishia yale wayatakayo. Basi hakika Mwenyezi Mungu atawamiminia rehema yake, kwani Yeye ni Mwenye kusamehe madhambi, Mwenye kuwarehemu viumbe vyake.

100 Na Waumini walio tangulia kusilimu, na Wahajiri (walio hama Makka kwenda Madina) na Ansari (wasaidizi wa Madina walio wapokea) walio kwenda mwendo mzuri wala hawakufanya taksiri, Mwenyezi Mungu yu radhi nao. Basi anawapokea na anawalipa mema. Na wao kadhaalika wameridhika na wamefurahia aliyo waandalia Mwenyezi Mungu, nayo ni Mabustani yapitayo mito kati ya miti yake. Wataneemeka humo kwa neema ya milele. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.

101 Na katika walio kuwa jirani na Madina miongoni mwa watu wa majangwani, walikuwako walio kuwa wakificha ukafiri wao na wakijidhihirisha kuwa ni Waumini. Na katika wakaazi wa Madina walikuwapo walio kuwa wamezoea unaafiki hata wakawa mabingwa, na wakawa wanauficha watu wasiutambue! Hata mwisho wewe, Mtume, usiwajue. Lakini Mwenyezi Mungu anajua hakika yao, na atawaadhibu duniani mara mbili - mara ya kwanza kwa kuwashinda maadui zenu, na hayo yatawaudhi wao; na mara nyingine kwa kuwafedhehi na kuwakashifu unaafiki wao. Tena, basi, watarejeshwa Siku ya Akhera kwenye adhabu ya Moto, na vitisho vyake vikubwa.

102 Na wapo watu wengine walio kuudhini, kisha baadae wakakubali makosa yao, na wakafuata Njia ya Haki. Basi watu hao wamefanya vitendo vyema na vitendo viovu. Kwa hao inatarajiwa kukubaliwa toba yao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwarehemu waja wake; huikubali toba yao na huwasamehe.

103 Ewe Mtume! Pokea kwa hawa wenye kutubu sadaka zao, uwasafishe kwa hizo sadaka makosa yao na uchoyo wao, na unyanyue daraja zao mbele ya Mwenyezi Mungu. Na waombe kheri na uwongofu; kwani kuomba kwako kutawapoza nafsi zao, na zitatulia nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia maombi, Mwenye kuwajua wenye nyoyo safi katika toba zao.

104 Hebu na wajue hao wanao tubu kuwa hakika Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anaye kubali toba ya kweli, na sadaka iliyo safi, na kwamba Yeye *Subhanahu* ndiye Mkunjufu wa fadhila katika kukubali toba, Mkuu katika kuwarehemu waja wake.

105 Ewe Mtume! Waambie watu: Tendeni wala msifanye taksiri katika vitendo vya kheri na kutekeleza waajibu. Kwani hakika Mwenyezi Mungu anavijua vitendo vyenu vyote. Na Mtume na Waumini nao pia wataviona na watavipima kwa vipimo vya Imani, na wataviona kwa mujibu wa itakikanavyo. Kisha mtarudishwa baada ya kufa kwa Mwenye kujua siri yenu na dhaahiri yenu, apate kukulipeni kwa vitendo vyenu, baada ya kukwambieni dogo lake na kubwa lake.

106. Na wapo wengine wanangojea amri ya Mwenyezi Mungu - ama atawaadhibu au atawasamehe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.¹⁰⁶

107. Na wapo walio jenga msikiti kwa ajili ya madhara na ukafiri na kuwafarikisha Waumini, na pa kuvizia kwa walio mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake hapo kabla. Na bila ya shaka wataapa kwamba: Hatukukusudia ila wema tu. Na Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa wao ni waongo.¹⁰⁷

108. Usisimame kwenye msikiti huo kabisa. Msikiti ulio jengwa juu ya msingi wa uchamngu tangu siku ya mwanzo unastahiki zaidi wewe usimame ndani yake. Humo wamo watu wanao penda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wanao jitakasa.¹⁰⁸

109. Je! Mwenye kuweka msingi wa jengo lake juu ya kumcha Mwenyezi Mungu na radhi zake ni bora au mwenye kuweka msingi wa jengo lake juu ya ukingo wa shimo linalo burugunyika, na likaburugunyika naye katika Moto wa Jahannamu? Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.¹⁰⁹

110. Na jengo lao hilo walilo lijenga litakuwa sababu ya kutia wasiwasi nyoyoni mwao mpaka nyoyo zao hizo zikatike vipande vipande. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.¹¹⁰

111. Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu - wanauwa na wanauwawa. Hii ni ahadi aliyo jilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur'ani. Na nani atimiza ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyo fanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa,¹¹¹

106 Na wapo watu wengine wametumbukia katika madhambi - wameacha kwenda kwenye Jihadi, lakini hawana unaafiki. Watu hawa wanangojea amri ya Mwenyezi Mungu. Ama awaadhibu au awakubalie toba yao awasamehe. Na Mwenyezi Mungu anazijua hali zao, na yaliyomo ndani ya nyoyo zao. Naye ni Mwenye hikima kwa ayafanyayo kwa waja wake, ikiwa kuwalipa thawabu au adhabu.

107 Na miongoni mwa wanaafiki walikuwapo jamaa walio jenga msikiti si kwa kutafuta ridhaa ya Mwenyezi Mungu, bali wakikusudia madhara, na kufuru, na kuwagawa Waumini. Na wao wataapa kuwa wao hawakutaka kwa kujenga msikiti huo ila kheri na a'mali njema. Na Mwenyezi Mungu anawashuhudia kuwa ni waongo katika hiyo Imani yao. (Tazama Maelezo 9:107)

108 Ewe Mtume! Usisali kabisa katika msikiti huo. Msikiti unao faa kupata rehema za Mwenyezi Mungu na radhi zake tangu mwanzo kama Masjid Qubaa ndio unao stahiki kusimamishwa ndani yake ibada za Mwenyezi Mungu. Katika msikiti huo wamo watu wanao penda kujinadhifisha miili yao na nyoyo zao kwa kutekeleza ibada zilizo sawa. Na Mwenyezi Mungu anawapenda na anawalipa thawabu wanao jikaribisha kwake kwa kujit'ahirisha nje na ndani, kiwiliwili na kiroho.

109 Hawi sawa katika itikadi yake wala katika vitendo vyake mwenye kusimamisha jengo lake kwa usafi wa niya katika kumcha Mwenyezi Mungu na kutafuta radhi zake, na yule mwenye kusimamisha jengo lake juu ya unaafiki, na ukafiri. Kwani vitendo vya mchamngu vimenyooka, vimejengeka juu ya msingi madhbuti. Na vitendo vya mnaafiki ni kama jengo lililo jengwa juu ya ukingo wa shimo. Jengo hilo litaporomoka tu, na litamtupa mwenyewe katika Moto wa Jahannamu. Na Mwenyezi Mungu hamuongoi kwenye Njia ya Uwongofu anaye shikilia kujidhulumu nafsi yake kwa ukafiri.

110 Na hilo jengo lao walilo lijenga wanaafiki litakuwa ni sababu ya kuwakereketa na kuwatia khofu katika nyoyo zao. Hayeshi hayo mpaka zipasuke nyoyo zao kwa majuto na kutubu au wafe! Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu, na Mwenye hikima katika vitendo vyake na malipo yake.

111 Mwenyezi Mungu anatilia mkazo ahadi yake aliyo wapa Waumini wanao toa nafsi zao na mali yao kwa ajili ya Njia yake, kuwa hakika Yeye amenunua kwao hizo nafsi zao na mali yao kwa kuwalipa Pepo kuwa ndio thamani ya hivyo walivyotoa. Kwani wao wanapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Wanawauwa maadui wa Mwenyezi Mungu, au wao wanakufa mashahidi katika Njia yake. Na Mwenyezi Mungu amethibitisha ukweli huu katika Taurati na Injili, kama alivyo thibitisha katika Qur'ani.

112. (Kwa) wanao tubia, wanao abudu, wanao himidi, wanao kimbilia kheri, wanao rukuu, wanao sujudu, wanao amrisha mema na wanao kataza maovu, na wanao linda mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na wabashirie Waumini.¹¹²

113. Haimpasii Nabii na wale walio amini kuwatakia msamaha washirikina, ijapo kuwa ni jamaa zao, baada ya kwisha bainika kuwa hao ni watu wa Motoni.¹¹³

114. Wala haikuwa Ibrahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu wa ahadi aliyo fanya naye. Lakini ilipo mbainikia kwamba yeye ni adui ya Mwenyezi Mungu, alijiepusha naye. Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, mnyenyekevu, mvumilivu.¹¹⁴

115. Na haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwahisabu watu kuwa wamepotea baada ya kwisha waongoza mpaka awabainishie ya kujiepusha nayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.¹¹⁵

116. Hakika Mwenyezi Mungu anao ufalme wa mbingu na ardhi; huhuisha na hufisha. Nanyi hamna Mlinzi wala Msaidizi isipo kuwa Mwenyezi Mungu.¹¹⁶

117. Mwenyezi Mungu amekwisha pokea toba ya Nabii na Wahajiri na Ansari walio mfuata katika saa ya dhiki, pale baada ya kukaribia nyoyo za baadhi yao kugeuka. Basi akapokea toba yao, kwani hakika Yeye kwao wao ni Mpole na ni Mwenye kuwarehemu.¹¹⁷

118. Na pia wale watatu walio achwa nyuma hata dunia wakaiona dhiki juu ya

Wala hapana yeyote mwenye kumshinda Mwenyezi Mungu katika kutimiza ahadi. Basi furahini, enyi Waumini Mujaahidina, kwa biashara hii mlio uza nafsi zenu na mali yenu ambayo yatatoweka, na badala yake mkanunua Pepo itakayo baki milele. Na biashara hii ndio ushindi mkubwa kwenu.

112 Sifa za wale walio uza nafsi zao kwa ajili ya Pepo ni kuwa wanakithirisha toba kwa Mwenyezi Mungu kwa kujikwaa kwao, na wanamhimidi katika kila hali, na wanakimbilia kwenda kujifanyia kheri nafsi zao na kuwafanyia wenginewe, na wanahifadhi Sala zao, na wanazitimiza kwa ukamilifu na unyenyekevu, na wanaamrisha kila kheri inayo wafikiana na Sharia ya Mwenyezi Mungu, na wanakataza kila uovu unao zuliwa na Dini, na wanaishika Sharia ya Mwenyezi Mungu. Ewe Mtume! Wabashirie kheri Waumini!

113 Haimfalii Nabii na Waumini kuwatakia maghfira washirikina, hata ikiwa ni jamaa zao wa karibu kabisa, baada ya kwisha hao Waumini kuwajua kwamba hao washirikina wamekufa katika ukafiri. Kwani hao wamestahiki kukaa milele Motoni.

114 Haikuwa vile alivyo fanya Ibrahim a.s. kumtakia msamaha baba yake ila ni kutimiza ahadi aliyo ahidi Ibrahim kumuahidi baba yake, kwa kutaraji kuwa atakuja amini. Ilipo kwisha mbainikia Ibrahim kuwa huyo ni adui wa Mwenyezi Mungu kwa kushikilia kwake ushirikina mpaka akafa na ukafiri, Ibrahim alijitenga naye, na akaacha kumwomba maghfira. Na Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, na mstahamilivu kwa maudhi.

115 Na si katika mwendo wa Mwenyezi Mungu na upole wake kwa waja wake kuwachukulia watu kuwa wamepotea, na awapitishie hukumu ya kuwatia khatiani na kuwapa adhabu, baada ya kwisha waongoza njia ya Uislamu, mpaka awabainishie kwa njia ya wahyi, ufunuo, kwa Mtume wake mambo ambayo inawapasa wajiepushe nayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua vyema kila kitu.

116 Hakika ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mmiliki wa mbingu na ardhi na viliomo ndani yake. Na Yeye ndiye Mwenye kuvisarifu viliomo humo kwa uhai na mauti. Na nyinyi hamna ila Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa kutawala mambo yenu, wala hamna Msaidizi mwingine wa kukunusuruni na kukulindeni.

117 Mwenyezi Mungu *Subhanahu* amemfadhili Nabii wake na Masahaba wake wenye kuamini, walio wakweli, miongoni mwa Wahajiri na Ansari, walio toka pamoja naye kwenda pigana Jihadi wakati wa shida. (katika vita vya Tabuk) (1). Aliwaweka imara na akawalinda wasikhitalifiane, baada ya shida ya dhiki ya kuwafarikisha baina yao, hata zikakaribia nyoyo zao kuelekea kutaka kubaki nyuma wasitoke kwenda kwenye Jihadi. Tena Mwenyezi Mungu aliwasamehe kwa ile raghba yao iliyo wapitia ndani ya nafsi zao. Hakika Yeye *Subhanahu* ni Mwenye upole mwingi, na Mwenye rehema kubwa. (*Tazama Maelezo 9:117*)

ukunjufu wake, na nafsi zao zikabanika, na wakayakinika kuwa hapana pa kumkimbia Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwake Yeye. Kisha akawaelekea kwa rehemu yake ili nao waendeleo kutubu. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu.¹¹⁸

119. Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli.¹¹⁹

120. Haiwafalii watu wa Madina na Mabedui walio jirani zao kubakia nyuma wasitoke na Mtume, wala kujipendelea nafsi zao kuliko yeye. Hayo ni kwa kuwa hakiwapati kiu, wala machofu, wala njaa, kwa ajili ya Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawendi mahali panapo waghadhibisha makafiri, wala hakiwapati chochote kutokana na maadui, ila huandikiwa kuwa ni kitendo chema. Hakika Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa wanao fanya mema.¹²⁰

121. Wala hawatoi cha kutoa kidogo wala kikubwa, wala hawalivuki bonde, ila huandikiwa, ili Mwenyezi Mungu awalipe bora ya waliyo kuwa wakiya tenda.¹²¹

122. Wala haiwafalii Waumini kutoka wote. Lakini kwa nini hawatoki baadhi katika kila kundi miongoni mwao, wakajifunze vyema Dini, na kisha waje kuwaonya wenzao watakapo warejea, ili wapate kujihadharisha?¹²²

123. Enyi mlio amini! Piganeni na wale makafiri walio karibu yenu, na wakute ugumu kwenu. Na jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wacha-Mngu.¹²³

124. Na inapo teremshwa Sura wapo miongoni mwao wasemao: Ni nani miongoni mwenu Sura hii imemzidishia Imani? Ama wale walio amini inawazidishia Imani, nao wanafurahi.¹²⁴

118 Na pia Mwenyezi Mungu aliwafadhili wale wanaume watatu walio baki nyuma wasitoke kwenda kwenye Jihadi katika vita vya Tabuk. Hawa hawakubaki nyuma kwa unaafiki. Ilikuwa inatarajiwa Mwenyezi Mungu atoe bayana ya hukumu yao. Iliyoy kuwa toba yao ni ya kweli, na majuto yao makubwa hata wakaiona dunia nyembamba juu ya upana wake, na nafsi zao zikaingwiwa na dhiki kwa hamu na huzuni, na wakajua kuwa hapana pa kuikimbia ghadhabu ya Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa kumwomba Yeye msamaha na kurejea kwake. Hapo basi Mwenyezi Mungu aliwaongoa watubu. Na Yeye akawasamehe, ili wapate kuendelea na hali ya toba. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kukubali toba za wenye kutubu, ni Mwingi wa kuwarehemu waja wake.

119 Enyi mlio amini! Simameni imara baraabara juu ya uchamngu na Imani. Na kuweni pamoja na wale walio wakweli katika kauli yao na vitendo vyao.

120 Haikuwa ni halali kwa wakaazi wa Madina na majirani zao katika wakaazi wa majangwani kubaki nyuma wasitoke kwenda vitani pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. Wala kujifanyia uchoyo kwa ajili ya nafsi zao katika aliyoy jitolea Mtume nafsi yake. (Mtume kajitolea roho na mali kwa kupigania Haki.) Kwani wao hakiwapati, katika Njia ya Mwenyezi Mungu, kiu, au machofu, au njaa, wala hawashuki pahala panapo watia ghadhabu makafiri, wala hakiwasibu kutokana na adui chochote kama kushindwa au kunyan'ganywa ngawira, ila huhisabiwa kwa hayo yote kuwa ni a'mali njema, ya kulipiwa bora ya malipo. Na Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa wenye kufanya mema katika vitendo vyao.

121 Na kadhaalika Mujaahidina hawatoi mali wanayo toa, kingi na kidogo, wala hawasafiri safari yoyote, kwa Njia ya Mwenyezi Mungu ila huandikiwa katika madaftari ya vitendo vyao vyema, ili wapate malipo wanayo stahiki kuyapata hao watendao.

122 Haifai Waumini watoke wote kwenda kwa Mtume s.a.w. ila iwe dharura. Itakikanavyo ni kutoka kikundi kwenda kwa Mtume kwa ajili ya kusoma Dini, na wapate kuwaita watu wao kuwaonya na kuwabashiria, pale wanapo rejea. Haya ili wapate kuwa imara daima juu ya Haki, na watahadhari na upotovu na uharibifu.

123 Enyi mlio amini! Piganeni na makafiri walio karibu yenu ili wasiwe ndio sababu ya kukutieni khatarini. Na kueni wakali kwao mnapo pigana, wala msiwafanyie upole. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu kwa msaada wake na nusra yake yu pamoja na wanao mcha.

124 Na ikiteremka Sura ya Qur'ani wakaisikia wanaafiki huifanyia maskhara na kuikejeli. Huambizana

125. Ama wale wenye maradhi katika nyoyo zao, basi inawazidishia uovu juu ya uovu wao; na wanakufa hali ni makafiri.¹²⁵

126. Je! Hawaoni ya kwamba wanatiwa mtihanini kila mwaka mara moja au mara mbili? Kisha hawatubu, wala hawakumbuki.¹²⁶

127. Na ikiteremka Sura hutazamana wao kwa wao, (kama kwamba wanasema:) Je! Yuko mtu anakuoneni? Kisha hugeukilia mbali. Mwenyezi amezigeuza nyoyo zao kwa kuwa hao ni watu wasio fahamu.¹²⁷

128. Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.¹²⁸

129. Basi wakigeuka, wewe sema: Mwenyezi Mungu ananitosheleza. Hapana mungu isipokuwa Yeye tu. Mimi namtegemea Yeye, na Yeye ndiye Mola Mlezi wa Kiti Kikuu cha Enzi.¹²⁹

wao kwa wao: Nani katika nyinyi iliyo mzidisha Imani? Ndio Mwenyezi Mungu anawajibu ya kwamba ipo farka baina ya wanaafiki na Waumini. Ama Waumini ndio wale walio iona Nuru na wakaijua Haki. Hao Aya za Mwenyezi Mungu zimewazidishia Imani, na wao huzifurahia wakati zinapo teremka.

125 Ama wanaafiki ambao nyoyo zao zinaugua, na macho yao yamepofoka, hao haziwazidishi ila ukafiri juu ya ukafiri walio nao, na watakufa hali nao ni makafiri.

126 Je! Hawazingatii wanaafiki vile Mwenyezi Mungu anavyo wapa majaribio kila mwaka mara moja au zaidi, kwa balaa namna mbali mbali, kama kuwakashifu siri zao, na kudhihirisha hali zao na kushindwa na Waumini, na kufichuliwa upotovu wao? Kisha juu ya yote hawaachi hao walio nayo wakatubu, wala hawayakumbuki yanao wapata.

127 Na kadhaalika ikiteremka Sura nao wapo barazani kwa Mtume hukonyezana na kuambiana: Yuko mtu anaye kuoneni? Tena nyoyo zao hukengeuka wasimfuata Mtume wala wasimuamini! Mwenyezi Mungu amewazidisha kupotea kwa vile kushikilia kwao kubaki katika upotovu na kuikataa Haki, kwani watu hawa hawafahamu kitu!

128 Enyi watu! Amekujieni Mtume, binaadamu kama nyinyi kwa umbo lake. Anapata dhiki kwa madhara yanayo kusibuni, ana hamu mwongoke, na mwingi wa huruma na rehema kwa Waumini.

129 Basi, ewe Mtume! Wakiipuza Imani, wakaikataa, wewe usihzunike kwa mapuuzo yao. Wewe tafakhari na utukufu wa Mola wako Mlezi, na useme: Ananitosheleza Mwenyezi Mungu, ambaye hapana mungu asiye kuwa Yeye. Juu yake Yeye tu peke yake mimi nategemea. Na Yeye ndiye Mmiliki wa ufalme wote, Mola Mlezi wa viumbe vyote, na ndiye Mwenye utawala mkuu.

Sura 10 - Yunus

Utangulizi

Sura hii ya Makka imeteremka Makka, na ina Aya 109. Imeanzia kuashiria cheo cha Kitabu hiki Kitukufu, na wasemayo washirikina yaliyo mkhusu Nabii s.a.w. Kisha ikataja ulimwengu na ishara za Mwenyezi Mungu Mtukufu ziliomo humo, na malipo ya Siku ya Kiyama, na mwendo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwatendea makafiri, na kuwakemea kwake kwa hizo itikadi zao, na hali ya watu wakati wa shida na neema, na uwezo wa Mwenyezi Mungu juu ya kila kitu, na kuemewa masanamu kufanya lolote. Na katika Sura hii wanatakiwa kama wanaweza makafiri waletе Sura japo moja ya kuzua. Na pia ndani yake kuna vitisho vikali vya adhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hali za nafsi za watu, na vipi Mwenyezi Mungu anavyo vichunguza vitendo vyao. Kisha baada ya hayo ikaingia kumwondolea Nabii s.a.w. kuungulika kwake kwa ukafiri wao, pamoja na kutoa hoja ya kuwavunja kabisa, na ikampoza kwa kumtaja hadithi za Manabii wengine na kaumu zao. Ikaja hadithi ya Nuhu, na hadithi ya Musa na Harun na Firauni na Wana wa Israili; kisha ikaashiriwa hadithi ya Yunus, na kwa jina hilo Sura hii ikaitwa. Na mwisho ikaelekea Sura hii kubainisha mambo ya Mtume huyu ili kutimiza mawaidha na mazingatio.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Ra. Hizo ni Aya za Kitabu chenye Hikima.¹
2. Je! Imekuwa ajabu kwa watu kwamba tumemfunulia mmoja wao kuwa: Waonye watu, na wabashirie wale walio amini ya kuwa watakuwa na cheo cha juu kwa Mola wao Mlezi? Wakasema makafiri: Hakika huyu ni mchawi dhaahiri!²
3. Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenyezi Mungu, ambaye ameziumba mbingu na ardhi kwa siku sita, na ametawala kwenye ufalme wake, anaendesha mambo yote. Hapana mwombezi ila baada ya idhini yake. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu Mlezi. Basi muabuduni Yeye. Je! Hamkumbuki?³

1 Harufi hizi - Alif Lam Raa - ni sawa na A.L.R. Mwenyezi Mungu Mtukufu imeanzia Sura hii. Na Yeye ndiye anajua muradi wake. Na juu ya hivyo zinaashiria kuwa Qur'ani imeundwa kwa harufi hizi hizi za Alifbete, na nyinyi mmeshindwa kuleta mfano wake! Na kwa harufi hizi za kutamkwa zinawazindua washirikina, wakawa wanasikiliza, ijapo kuwa wanawafikiana kuwa wasizisikilize Aya Tukufu hizi na mfano wake ambazo ni Aya za Qur'ani yenye hikima katika mpango wake na maana zake, na ambayo imekusanya hikima na kila linalo wanafuisha watu katika Dini yao na dunia yao

2 Haiwafalii watu kustaajabu wakakanusha wahyi wetu tunao mfunulia mtu mmoja wao, naye ni Nabii Muhammad s.a.w., ili awahadharishe watu na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na awape bishara njema wale miongoni mwao walio amini, ya kwamba hapana shaka yoyote wana cheo kitukufu cha juu kwa Mola wao Mlezi. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu haigeuki. Wala haiwafalii hao watu wakanushi kumsema Muhammad, Mtume wetu, kuwa yeye ni mchawi maarufu.

3 Enyi watu! Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenyezi Mungu aliye umba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake katika siku sita ambazo kipimo chake hakijui ila Mwenyezi Mungu. Akatandaza utukufu wa utawala wake, peke yake, na akayapanga mambo yote ya viumbe vyake. Basi hapana yeyote mwenye chochote pamoja na utawala wa Mwenyezi Mungu. Wala hawezi yeyote katika viumbe vyake hata kumwomba mtu isipo kuwa kwa ruhusa yake. Huyu, basi, ndiye Mwenyezi Mungu Muumba, huyo ndiye

4. Kwake Yeye tu ndio marejeo yenu nyote. Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo ya kweli. Hakika Yeye ndiye aliye anzisha uumbaji, na kisha ataurejesha ili awalipe kwa uadilifu wale walio amini na wakatenda mema. Na walio kufuru, wao watapata vinywaji vinavyo chemka, na adhabu chungu kwa sababu ya walivyo kuwa wakikufuru.⁴
5. Yeye ndiye aliye lijaalia jua kuwa na mwangaza, na mwezi ukawa na nuru, na akaupimia vituo ili mjue idadi ya miaka na hisabu. Mwenyezi Mungu hakuviumba hivyo ila kwa Haki. Anazipambanua Ishara kwa watu wanao jua.⁵
6. Hakika katika kukhitalifiana usiku na mchana, na katika alivyo umba Mwenyezi Mungu katika mbingu na ardhi, zipo Ishara kwa watu wanao mcha-Mngu.⁶
7. Hakika wasio taraji kukutana nasi, na wakaridhia maisha ya dunia na wakatua nayo, na walio ghafilika na Ishara zetu,⁷
8. Hao, makaazi yao ni Motoni kwa sababu ya waliyo kuwa wakiyachuma.⁸
9. Hakika walio amini na wakatenda mema, Mola wao Mlezi atawaongoa kwa sababu ya Imani yao. Itakuwa inapita mito kati yao katika Mabustani yenye neema.⁹
10. Wito wao humo utakuwa: *Subhanaka Llahumma* “Umetakasika Ee Mwenyezi Mungu!” Na maamkio yao humo ni “*Salama*”. Na mwisho wa wito wao ni: *Alhamdulillah Rabbi A’lamain* “Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.”¹⁰
11. Na lau kama Mwenyezi Mungu angeli wafanyia watu haraka kuwaletea shari kama

Mola wenu Mlezi, na ndiye Mlinzi wa neema zenu. Basi muabuduni Yeye peke yake, na msadikini Mtume wake, na kiaminini Kitabu chake. Juu yenu kukumbuka neema za Mwenyezi Mungu, na zingatieni Ishara zake zinazo thibitisha Upweke wake. (*Tazama* Maelezo 10:3)

4 Kama Mwenyezi Mungu alivyo anzisha uumbaji wa viumbe peke yake, basi marejeo yenu, na marejeo ya viumbe vyote ni kwake Yeye. Na Mwenyezi Mungu amehidi hivyo kwa ahadi ya kweli isiyo na khitilafu. Na hakika Yeye *Subhanahu* ameanzisha kuumba viumbe kwa kudra yake, na vitapo teketea atavirejesha kwa kudra yake, ili awalipe Waumini wenye kumt’ii thawabu kwa uadilifu ulio timia. Ama makafiri, wao huko katika Jahannamu watapewa vinywaji vinavyo tokota kweli kweli, na watapata adhabu yenye kutia machungu kuwa ni malipo ya ukafiri wao.

5 Na Mola wenu Mlezi ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi, na akalifanya jua litoe mwanga, na mwezi utoe nuru. Na akajaalia mwezi uwe na vituo ili vikusaidieni kuweza kupima nyakati zenu, na mjue idadi ya miaka na hisabu. Na wala Mwenyezi Mungu hakuumba hayo ila kwa hikima. Na Yeye *Subhanahu* katika Kitabu chake anazikunjua Ishara zenye kuonyesha Ungu wake na ukamilifu wa uwezo wake, ili mpate kuzingatia kwa akili zenu, na mkubali kwa yanayo hitajia ujuzi. (*Tazama* Maelezo 10:5)

6 Hakika katika kufuatana usiku na mchana na kukhitalifiana kwao, kwa kuzidi na kupungua, na katika uumbaji wa mbingu na ardhi na vitu vyote viliomo humo, zipo dalili zilizo wazi na hoja zilizo dhaahiri zenye kuhakikisha Ungu wa Mwenye kuumba, na uwezo wake. Hayo ni kwa wenye kutaka kuiepuka ghadhabu yake na wakaiogopa adhabu yake. (*Tazama* Maelezo 10:6)

7 Hakika wale wasio amini kufufuliwa na kukutana na Mwenyezi Mungu Siku ya Mwisho, na wakaamini - kwa kudhani tu - kuwa uhai wa duniani ndio mwisho wao na hapana baada yake uhai mwingine, na wakatulia nyoyo zao kwa hayo, na wala wasijue nini kitakuwa baada yake, na wakaghaflika na Ishara za Mwenyezi Mungu juu ya kufufuliwa na kuhisabiwa.

8 Watu hao, makaazi yao watakapo dumu ni Motoni. Hayo ni malipo kwa waliyo yachuma ya ukafiri na vitendo viovu.

9 Hakika walio amini Imani ya kweli kweli, na wakatenda mema katika dunia yao, Mola wao Mlezi atawathibitisha kwenye Uwongofu kwa sababu ya Imani yao, na Siku ya Kiyama atawatia katika Bustani zipitazo mito kati yake, na wataneemeka kwa neema za milele.

10 Dua za Waumini katika Bustani hizo ni kumsabihi na kumtakasa Mwenyezi Mungu na kila waliyo kuwa wakiyasema makafiri duniani, na kusalimiwa na Mwenyezi Mungu, na kusalimiana wao kwa wao ili kuthibitisha amani na utulivu. Na kukhitimishia dua yao ni kumhimidi Mwenyezi Mungu kwa tawfiqi yake, kuwawezesha, kufikia Imani na kufuzu kwao kuipata radhi yake.

wanavyo jihimizia kuletewa kheri, bila ya shaka wangelisha timiziwa ajali yao. Lakini tunawaacha wale wasio tumainia kukutana nasi wakihangaika katika upotovu wao.¹¹

12. Na mtu akiguswa na shida hutuomba naye kaegesha ubavu, au kakaa, au kasimama. Lakini tukimwondoshea shida yake huendelea kama kwamba hakupata kutuomba tumwondoshee shida iliyo mpata. Ndio namna hiyo wamepambiwa warukao mipaka yale waliyo kuwa wakiyatenda.¹²

13. Na kwa yakini tumekwisha ziangamiza kaumu za kabla yenu walipo dhulumu, na waliwajia Mitume wao kwa Ishara zilizo wazi; lakini hawakuwa wenye kuamini. Ndio kama hivyo tunavyo walipa watu wakosefu.¹³

14. Kisha tukakufanyeni nyiye ndio wenye kushika mahala pao baada yao katika ardhi ili tuone jinsi mtakavyo tenda.¹⁴

15. Na wanapo somewa Aya zetu zilizo wazi, wale wasio taraji kukutana na Sisi husema: Lete Qur'ani isiyo kuwa hii, au ibadilishe. Sema: Hainifalii mimi kuibadilisha kwa nitakavyo nafsi yangu. Mimi sifuati ila ninayo funuliwa kwa Wahyi. Hakika mimi naogopa, nikimuasi Mola wangu Mlezi, adhabu ya Siku iliyo kuu.¹⁵

16. Sema: Mwenyezi Mungu angeli taka nisingeli kusomeeni, wala nisingeli kujuvyeni. Kwani nalikwisha kaa nanyi umri mzima kabla yake! Basi, je! Hamzingatii?¹⁶

11 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli waitikia watu wanapo jiapizia shari kama vile wanavyo jihimizia kuitaka kheri, angeli waangamiza akawateketeza wote. Lakini Yeye anawachukulia kwa upole basi anaakhirisha kuwateketeza, ili kungojea wadhahirishe walio nayo kwa mujibu wa anavyo wajuulia, upate kuonekana wazi uadilifu wake kwa atavyo walipa. Wanaachwa na ushahidi wa kutosha umesimama dhidi yao, nao makusudi wanakengeuka na kuelekea njia ya upotovu na udhalimu.

12 Na mtu akisibiwa na madhara katika nafsi yake au mali yake au mfano wa hayo, huhisi unyonge wake, na humwomba Mola wake Mlezi kwa hali yoyote - akiwa kajinyoosha, au kakaa kitako, au kasimama - amwondolee dhiki zake! Mwenyezi Mungu akisha mwitikia, na akamwondolea hizo shida zake, humuacha kando Mwenyezi Mungu na akaendelea na maasi yake, na akasahau fadhila za Mwenyezi Mungu juu yake, kama kwamba hakupatikana na madhara yoyote, wala hajapata kumwomba amwondolee! Na mfano wa mtindo huu Shetani ndio huwazaini Makafiri, akawapambia vitendo vyao viovu, na uzushi wao mpotovu, wakaona yote hayo ni mazuri.

13 Na Sisi tulikwisha ziangamiza kaumu zilizo kutangulieni kwa sababu ya kufuru zao walipo wajia Mitume na Ishara zilizo wazi za kusadikisha wito wao wa kuitia Imani. Na Mwenyezi Mungu akijua, kwa ajili ya kung'ang'ania kwao ukafiri na uasi, kuwa haitopatikana Imani kwao! Basi enyi makafiri wa Kikureshi! Zingatieni! Kama tulivyo waangamiza walio kuwa kabla yenu, kadhaalika tutawalipa wakosefu kwa maangamizo.

14 Enyi Umma wa Muhammad! Tumekujaalieni muwe makhalifa wa ardhi, mshike pahala pa walio kutangulieni, ili tukujaribuni tudhahirishe mtacho kikhiari, ut'iifu au uasi, baada ya mlivyo kwisha juu yaliyo wapata walio kutangulieni.

15 Zilipo dhihiri Aya (Ishara) za Qur'ani kutokana na Mtume wetu Muhammad juu ya washirikina, walisema makafiri wasio ikhofu adhabu ya Mwenyezi Mungu wala hawataraji thawabu zake: Tuletete kitabu kinginecho kisicho kuwa hii Qur'ani. Au badilisha yaliyomo humu, yale yasiyo tupendeza. Waambie ewe Mtume: Hayumkini wala haijuzu mimi kugeuza au kubadilisha kwa nafsi yangu. Mimi si chochote ila ni mwenye kufuata na mwenye kufikisha kile kinacho funuliwa kwangu kutokana na Mola wangu Mlezi. Mimi naogopa, nikienda kinyume na Wahyi, Ufunuo, wa Mola wangu Mlezi, adhabu ya Siku ambayo khatari yake ni kuu, na kitisho chake ni kikubwa!

16 Waambie ewe Mtume! Lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka kuwa asiniteremshie Qur'ani kutoka kwake, wala mimi nisikufikishieni, asingeli teremsha, wala mimi nisingeli kusomeeni, na wala Mwenyezi Mungu asingeli kufundisheni. Lakini Yeye kateremsha, na kanituma mimi kwayo, na mimi nimekusomeeni kama alivyo niamrisha. Na mimi nilikwisha kaa nanyi wakati mrefu kabla ya kupewa Utume, na mimi sikudai Utume wakati huo, wala sikukusomeeni kitu chochote. Na nyinyi mmeshuhudia kuwa mimi ni mkweli na muaminifu. Lakini umekuja Ufunuo na nimeamrisha niusome. Basi hebu

17. Basi ni nani aliye dhaalimu zaidi kuliko yule anaye mzulia uwongo Mwenyezi Mungu na akazikanusha Ishara zake? Hakika hawafanikiwi wakosefu.¹⁷

18. Nao, badala ya Mwenyezi Mungu, wanaabudu wasio wadhuru wala kuwanufaisha, na wanasema: Hawa ndio waombezi wetu kwa Mwenyezi Mungu! Sema: Je! Mnamwambia Mwenyezi Mungu asiyo yajua ya katika mbingu wala katika ardhi? *Subhanahu wa Taa'la!* Ametakasika na ametukuka na hao wanao mshirikisha naye.¹⁸

19. Wala watu hawakuwa ila Umma mmoja tu. Kisha wakakhitalifiana. Na lau kuwa si neno lililo kwisha tangulia kutokana na Mola wako Mlezi, hapana shaka hukumu ingeli kwisha katwa baina yao katika hayo wanayo khitalifiana.¹⁹

20. Na wanasema: Kwa nini hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake Mlezi? Sema: Mambo ya ghaibu ni ya Mwenyezi Mungu. Basi nyinyi ngojeni, na mimi ni pamoja nanyi katika wanao ngojea.²⁰

21. Na tunapo waonjesha watu rehemba baada ya shida waliyo ipata, utawaona wana vitimbi kuzipangia Ishara zetu. Sema: Mwenyezi Mungu ni Mwepesi zaidi wa kupanga. Hakika wajumbe wetu wanayaandika mnayo yapanga.²¹

22. Yeye ndiye anaye kuendesheni bara na baharini. Hata mnapo kuwa majahazini na yakawa yanakwenda nao kwa upepo mzuri wakaufurahia, upepo mkali ukawazukia, na yakawajia mawimbi kutoka kila upande, na wakaona wamesha zongwa, basi hapo humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia niya: Ukituokoa na haya bila ya shaka

yatieni akilini haya mambo, na myazingatie, na yakutanisheni yaliyo pita ya zamani na ya yaliopo sasa.

17 Hapana mtu aliye jidhulumu nafsi zaidi kuliko anaye kufuru na akamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, au akazikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu alizo kuja nazo Mtume wake. Hakika hafuzu kafiri katika vitendo vyake. Naye amekhasiri khasara iliyo wazi kwa ukafiri wake na amemghadhibisha Mwenyezi Mungu.

18 Na hawa washirikina wanao mzulia Mwenyezi Mungu kuwa ana washirika, wanaabudu masanamu ya upotovu. Hayawadhuru wala hayawanufaishi. Na wanasema: Masanamu haya yatatuomba kwa Mwenyezi Mungu Siku ya Akhera! Ewe Mtume! Waambie: Hivyo nyinyi mnamwambia Mwenyezi Mungu kuwa ana washirika ambao hawajui, la katika mbingu wala katika ardhi? Mwenyezi Mungu ametakasika na kuwa na washirika, na yote mnayo zua kwa kuwaabudu hao washirika.

19 Watu kwa maumbile yao hawakuwa ila ni Umma mmoja tu. Kisha tukawapelekea Mitume wawaongoze na wawaongoe kwa mujibu wa Ufunuo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ikawa tabia ya kibinaadamu iliyo pelekea kheri na shari ndiyo sababu ya kuwa na nguvu zaidi shari katika baadhi yao. Juu yao hao matamania na nyendo za Shetani zikatawala, na kwa hivyo wakakhitalifiana. Na lau kuwa hukumu ya Mola wako Mlezi haikutangulia ya kuwapa muhula makafiri kwa ajili yako, Ewe Nabii, na kuakhirisha maangamizo yao mpaka siku maalumu iliyo ahidiwa, Mwenyezi Mungu angeli wapelekea upesi maangamizo na adhabu, kwa sababu ya mfarakano waliyo uingia, kama zilivyo ingia kaumu zilizo kwisha pita.

20 Na hawa washirikina wanasema: Hivyo Muhammad hateremshiwi muujiza usio kuwa hii Qur'ani, wa kutuyakinisha Utume wake? Waambie Ewe Mtume! Kuteremshwa Ishara ni jambo la ghaibu, hapana alijuaye ila Mwenyezi Mungu. Kama Qur'ani haikufaini basi ngojeni hukumu ya Mwenyezi Mungu baina yangu na nyinyi katika hayo mnayo yabisha. Na mimi ni pamoja nanyi katika wanao ngojea.

21 Katika mitindo ya watu ni kuwa pale tunapo waneemesha baada ya kwisha patwa na shida katika nafsi zao, au ahli zao (watu wao), au mali zao, hawamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema anazo waneemesha na kuwaondolea madhara. Bali huyakabili hayo kwa kukakamia katika kuzikadhibisha na kuzikataa Ishara za Mwenyezi Mungu! Ewe Mtume! Sema: Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kukuhilikini na kukuadhibuni upesi upesi, lau kuwa si hukumu yake tangu hapo kukupeni muhula mpaka siku ya miadi aliyo iweka mwenyewe kwa ilimu yake peke yake. Hakika Wajumbe wetu, Malaika waliyo wakilishwa juu yenu wanaviandika vitimbi mnavyo vipanga, na Yeye Mwenyezi Mungu atakuhisabieni na atakulipeni.

tutakuwa miongoni mwa wanao shukuru.²²

23. Lakini akisha waokoa, mara wanafanya jeuri tena katika nchi bila ya haki. Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe. Hii ni starehe ya maisha ya dunia tu. Kisha marejeo yenu ni kwetu, na hapo tutakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.²³

24. Hakika mfano wa maisha ya dunia ni kama maji tuliyo yateremsha kutoka mbinguni, kisha yakachanganyika na mimea ya ardhi wanayo ila watu na wanyama. Mpaka ardhi ilipo kamilika uzuri wake, na ikapambika, na wenyewe wakadhani wamesha iweza, iliifikia amri yetu usiku au mchana, tukaifanya kama iliyo fyekwa - kama kwamba haikuwapo jana. Namna hivi tunazipambanua Ishara zetu kwa watu wanao fikiri.²⁴

25. Na Mwenyezi Mungu anaita kwendea Nyumba ya Amani, na anamwongoa amtakaye kwenye Njia Iliyo Nyooka.²⁵

26. Kwa wafanyao wema ni wema na zaidi. Wala vumbi halitawafunika nyuso zao, wala madhila. Hao ndio watu wa Peponi. Humo watadumu.²⁶

27. Na wale walio chuma maovu, malipo ya uovu ni mfano wake vile vile, na yatawafika madhila. Hawatakuwa na wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu. Nyuso zao kama kwamba zimefunikwa na vipande vya usiku wa giza. Hao ndio watu wa Motoni, wao humo watadumu.²⁷

22 Mwenyezi Mungu mnaye ikufuru neema yake, na mnakanusha Ishara zake, ndiye Yeye anaye kuezesheni kwenda na kutembea nchi kavu kwa miguu au kwa vipando, na baharini kwa vyombo alivyo fanya vikutumikieni, vinavyo kwenda juu ya maji, kama anavyo visahilishia Mwenyezi Mungu kwa upepo mzuri unao puliza kwa amani mpaka kufikilia huko vyendako. Hata mkisha tumaini na mkafurahia huvuma tena upepo mkali ukatibua mawimbi kutoka kila upande, na mkayakinika kuwa hapana ila kuhiliki tu! Katika shida kama hii hamna tegemeo ila Mwenyezi Mungu. Hapo basi mnamwomba madua kwa usafi wa niya, kwa kuyakinika kuwa hapana mwokozi isipo kuwa Yeye, na mnampa ahadi kuwa pindi akikuvueni na balaa hiyo mtamuamini, na mtakuwa wenye kushukuru.

23 Na akisha waokoa kutokana na khatari ya kuteketea, wanavunja ahadi yao, na mara wanarejea kwenye fisadi walizo kuwa nazo kabla! Enyi watu mvunjao ahadi! Hakika matokeo ya kupindukia mipaka ya starehe na kudhulumu kwenu yatarejea juu yenu peke yenu. Na hakika hizo starehe mnazo zistarehea katika dunia yenu ni starehe za kidunia zenye mwisho. Kisha marejeo yenu ya mwisho ni kwa Mwenyezi Mungu, na Yeye atakulipeni kwa vitendo vyenu mliwyo vitanguliza duniani.

24 Hakika hali ya uhai wa dunia kwa uzuri wake na starehe zake, na kisha baada ya hayo kutoweka, si chochote ila ni kama hali ya maji yanayo teremka mbinguni, yakachanganyika na mimea ya ardhi inayo liwa na watu na wanyama. Mimea hiyo ikastawi na ikatoa matunda, na ardhi ikapambika kwa kunawiri. Uzuri huo ukisha fika ukomo wake, na wenyewe wakayakinika kuwa kweli ni mali yao, na kuwa watanafiika kwa matunda yake na neema zake, amri yetu ya kuondoa yote hayo ikaja. Tukaifanya kama kwamba iliyo fyekwa, na kama kwamba haijapata kukaliwa wala haikupata kuwa na uzuri kabla yake! Na hali zote mbili za kustawi na kunawiri ya kufurahia watu na kinyume cha hayo, ni mambo ya kuondoka na kutoweka! Na kama alivyo bainisha Mwenyezi Mungu kwa mifano iliyo wazi, anabainisha Aya zake na anafafanua hukumu zake na Ishara kwa watu wanao fikiri na wanapima kwa akili. (*Tazama Maelezo 10:24*)

25 Na Mwenyezi Mungu anawaitia waja wake kwa Imani na vitendo vyema wende Peponi, makao ya amani na utulivu. Na Yeye *Subhanahu* humwongoa amtakaye - kwa kuwa kesha jitayarisha vyema na kaelekea kheri - kwenye Njia ya Haki, nayo ni ya Salama.

26 Wanao tenda mema kwa kuitikia Wito wa Mwenyezi Mungu, wakaamini na wakafanya kheri kwa Dini yao na dunia yao, hao watapata wema katika Akhera, na wema huo ni Pepo. Na tena watapata yaliyo zidi hayo kwa fadhila na ukarimu wa Mwenyezi Mungu. Wala nyuso zao hazitafunikwa na huzuni na hamu na fedheha. Hawa ndio watu wa Peponi watakao neemeka humo daima milele.

27 Na wale ambao hawakuitikia Wito wa Mwenyezi Mungu, wakakufuru, wakatenda maasi, watalipwa kwa mujibu ya uovu walio utenda. Na hawana mlinzi wa kuwakinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na nyuso zao zitasawajika kwa ghamu na huzuni kama kwamba zimefunikwa na weusi wa kiza cha usiku!

- 28.** Na siku tutakapo wakusanya wote, kisha tutawaambia walio shirikisha: Simameni mahali penu nyinyi na wale mlio wafanya washirika. Kisha tutawatenga baina yao. Na hao walio washirikisha watasema: Nyinyi hamkuwa mkituabudu sisi.²⁸
- 29.** Mwenyezi Mungu anatosha kuwa ni shahidi baina yetu na nyinyi. Hakika sisi tulikuwa hatuna khabari ya ibada yenu.²⁹
- 30.** Huko kila mtu atayajua aliyo yatanguliza. Na watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki, na yote waliyo kuwa wakiyazua yatawapotea.³⁰
- 31.** Sema: Ni nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Au ni nani anaye miliki kusikia na kuona? Na nani amtoaye hai kutoka maiti, na akamtoa maiti kutoka aliye hai? Na nani anaye yadabiri mambo yote? Watasema: Allah, Mwenyezi Mungu. Basi sema: Je! Hamchi?³¹
- 32.** Basi huyo ndiye Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu wa haki. Na kipo kitu gani baada ya haki, isipokuwa upotovu tu? Basi huwaje mkageuzwa?³²
- 33.** Ndio kama hivyo kauli ya Mola wako Mlezi itakavyo wathibitikia wale walio potoka, ya kwamba hawatoamini.³³
- 34.** Sema: Je! Yupo katika miungu yenu ya ushirikina aliye anzisha kuumba viumbe, na kisha akavirejesha? Huwaje, basi, mkadanganywa?³⁴

Na hao ndio watu wa Motoni, watasononeka humo milele.

28 Ewe Mtume! Kumbuka kitisho cha siku watapo kusanywa viumbe vyote, kisha tuwaambie walio mshirikisha Mwenyezi Mungu katika ibada zao: Simameni pahala penu nyinyi na hao mlio wafanya washirika wa Mwenyezi Mungu, muangalie mtafanywa nini? Patatokea mfarakano baina ya washirikina na hao miungu yao ya uwongo walio washirikisha na Mwenyezi Mungu. Hao miungu watajitenga na wale wafwasi wao, kwa kusema: Sisi hatukukutakeni mtuabudu. Wala nyinyi hamkuwa mkituabudu sisi! Hakika mlikuwa mkiyaabudu matamano yenu tu.

29 Mwenyezi Mungu anatosheleza kwa ilimu yake na hukumu yake kuwa ni Shahidi wa kutupambanua baina yetu na nyinyi. Sisi tulikuwa mbali nanyi, wala hatukuwa tunafaidika vyovyote kwa huko kutuabudu kwenu.

30 Katika msimamo huo kila mtu atajua kheri gani au shari gani aliyo ifanya, na atalipwa malipo yake. Na hapo hao washirikina watayakinika kuwa kweli Mwenyezi Mungu ni Mmoja na wa pekee, Mwenye Haki. Na yote waliyo kuwa wakimzulia Mwenyezi Mungu yatavunjika.

31 Ewe Mtume! Lingania kwenye Tawhidi safi, na useme: Nani anaye kuleteeni riziki kutoka mbinguni inapo teremka mvua, na katika ardhi inapo mea mimea na kuzaa? Na nani aliye kupeni kusikia na kuona? Na nani anaye toa vilio hai kutokana na vilio maiti, kama mimea, nayo ni hai kutokana na ardhi maiti? Nani anaye mtoa maiti kutokana na hai, kama mtu anavyo kufa? Na nani anaye panga na kuendesha mambo yote ya ulimwengu kwa kudra yake na hikima yake? Wataungama: Hapana pa kukimbilia! Kwa hakika ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mtenda yote. Ewe Mtume! Waambie watapo ungama: Si waajibu mkubwa kuit'ii Haki, na kumkhofu Mwenyezi Mungu, Mmiliki Ufalme wote.

32 Huyo basi ndiye Mwenyezi Mungu mliye mkiri, na Yeye tu peke yake ndiye Mola wenu Mlezi aliye thibiti kuwa ni Mola na Mlezi, na akapasa kuabudiwa pekee, wala hapana mwenginewe. Na hapana baada ya Haki ya Umoja wa Mwenyezi Mungu na kumuabudu Yeye tu, ila kutumbukia katika upotovu, nao ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kumuabudu mwenginewe. Basi vipi mnaicha Haki mkauendea upotovu?

33 Kama ulivyo thibiti Ungu wa Mwenyezi Mungu na kumuabudu Yeye, vile vile imethibiti hukumu juu ya walio tokana na amri ya Mwenyezi Mungu wakimuasi kwa kuwa hawafuati Haki. Kwani hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hawaongoi kwenye Haki ila wanao ishika njia yake, sio wanao mfanyia uasi.

34 Ewe Mtume! Waambie hao washirikina: Yupo yeyote katika hao mlio wafanya washirika wa Mwenyezi Mungu mkawaabudu, awezaye kuanzisha kuumba tangu mwanzo, na tena akarejea tena baada ya kwisha toweka? Hapana shaka watashindwa kujibu! Basi hapo tena waambie: Allah, Mwenyezi Mungu, tu peke yake, ndiye anaye anzisha kuumba kutokana na kuto kuwepo, na tena viumbe vikitoweka huvirejesha. Vipi basi nyinyi mnaicha Imani?

35. Sema: Je! Yupo katika miungu yenu ya ushirikina anaye ongoa kwendea Haki? Sema: Mwenyezi Mungu anaongoa kwendea Haki. Basi, je, anaye stahiki kufuatwa ni yule Mwenye kuongoa kwendea Haki au asiye ongoa ila aongozwe yeye? Basi nyinyi mna nini? Mnahukumu namna gani?³⁵

36. Na wengi wao hawafuati ila dhana tu. Na dhana haifai kitu mbele ya haki. Hakika Mwenyezi Mungu anajua yote wanayo yatenda.³⁶

37. Na haiwezekani Qur'ani hii kuwa imetungwa na haitoki kwa Mwenyezi Mungu. Lakini hii inasadikisha yaliyo tangulia, na ni mfafanuo wa Kitabu kisicho na shaka ndani yake, kutokana na Mola Mlezi wa viumbe vyote.³⁷

38. Je! Ndiyo wanasema ameizua? Sema: Hebu leteni sura moja mfano wake na muwaite (kukusaidieni) muwawezao, isipo kuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnasema kweli.³⁸

39. Bali wameyakanusha wasio yaelewa ilimu yake kabla hayajawajia maelezo yake. Kadhaalika walio kabla yao walikanusha vile vile. Basi angalia jinsi ulivyo kuwa mwisho wa madhaalimu hao.³⁹

40. Na miongoni mwao wapo wanao iamini, na miongoni mwao wapo wasio iamini. Na Mola wako Mlezi anawajua vyema mafisadi.⁴⁰

41. Na wakikukanusha wewe, sema: Mimi nina a'mali yangu, na nyinyi mna

35 Ewe Mtume! Waambie hao washirikina: Yupo yeyote katika hao mlio wafanya washirika wa Mwenyezi Mungu mkawaabudu, awezaye kupambanua baina ya uwongofu na upotovu, akawaongoza watu kwenye Njia ya Haki? Wataemewa! Basi, je! Yupi bora kufuatwa - Mwenye kuweza kuongoa kwendea Haki au asiye weza hata kujiongoa nafsi yake? Naye huyo havezi kumwongoa mtu, ila yeye anahitaji mtu wa kumwongoa. Hao ndio kama wakuu wa makafiri, mapadri na mamonaki ambao ndio mmewafanya ni waola mkamuacha Mwenyezi Mungu!! Nini basi kilicho kupelekeeni kukengeuka hata mkawashirikisha hawa na Mwenyezi Mungu? Na nini hali ya ajabu iliyo kusukumeni kwenye hizo hukumu na sharia za kigeni?

36 Wengi wa washirikina hawafuati katika itikadi zao ila dhana potovu zisio kuwa na dalili zozote! Na kwa jumla, dhana haifidi kitu, wala haiwezi kuwa ni badala ya kuijua Haki, na khasa ikiwa dhana yenyewe ni ya kuzua tu, kama hizi dhana za washirikina. Na hakika Mwenyezi Mungu anajua vyema wayafanyayo wakuu wa ukafiri na wafuasi wao, naye atawalipa kwa hayo.

37 Haiwezi kutokea kuwa hii Qur'ani aizue mtu yeyote, kwani katika kuwa haiwezi kuigwa, na katika uwongofu wake, na hukumu zake, hayumkini kuwa itoke kwa yeyote isipo kuwa kwa Mwenyezi Mungu tu. Nayo inasadikisha Vitabu vya mbinguni vilivyo tangulia katika mambo ya Haki yaliyo tajwa humo, na inaweka wazi yaliyo kwisha andikwa na kuthibitisha katika mambo ya hakika na sharia. Hapana shaka kuwa Qur'ani hii ina cheo maalumu kwa Mwenyezi Mungu, nayo ni muujiza ambao hapana mtu anaye weza kuleta mfano wake.

38 Bali hawa washirikina wanasema: Muhammad kaizua hii Qur'ani mwenyewe! Ewe Mtume! Waambie: Ikiwa hii Qur'ani ni kazi ya mwanaadamu, basi nyinyi leteni Sura moja tu mfano wake, na muwatake muwatakao, isipo kuwa Mwenyezi Mungu, waje kukusaidieni; ikiwa nyinyi ni wasema kweli katika madai yenu kuwa hii Qur'ani nimeitunga mimi.

39 Bali hawa washirikina wamekimbilia kuikadhibisha Qur'ani bila ya kuzingatia, wakajua yaliomo ndani yake! Wao wenyewe hawakutazama mna nini, wala hawakusita kuitafuta tafsiri yake, na kutaka kuelewa hukumu zake kwa kuwauliza wenginewe! Na kukadhibisha namna hii bila ya ujuzi, ndivyo walivyo wakanusha makafiri wa kaumu za zamani Mitume wao na Vitabu vyao! Basi, ewe mwanaadamu! Angalia yaliishiaje mambo ya walio kadhibisha walio tangulia. Waliachiliwa mbali na wakateketezwa kwa adhabu! Na huu ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu kwa mfano wa hao.

40 Na miongoni mwa hawa wakanushao wapo ambao watakuja iamini Qur'ani baada ya kuyafahamu yaliyomo ndani yake, na wakayaelewa maana yake. Na kipo miongoni mwao kikundi ambacho hakiamini wala hakiachi upotovu wake! Na Allah *Subhanahu wa Taa'la* anawajua vyema wakanushao mafisadi, na atawalipa kwa vitendo vyao.

a'mali yenu. Nyinyi hamna jukumu kwa niyatendayo, wala mimi sina jukumu kwa myatendayo.⁴¹

42. Na wapo miongoni mwao wanao kusikiliza. Je, wewe unaweza kuwafanya viziwi wasikie ijapo kuwa hawafahamu?⁴²

43. Na wapo miongoni mwao wanao kutazama. Je, wewe utawaongoa vipofu ingawa hawaoni?⁴³

44. Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu kitu chochote; lakini watu wenyewe wanajidhulumu nafsi zao.⁴⁴

45. Na Siku atakapo wakusanya, itakuwa kama kwamba hawakukaa ila saa moja tu ya mchana! Watatambuana. Hakika wamekhasirika walio kanusha kukutana na Mwenyezi Mungu, wala hawakuwa wenye kuongoka.⁴⁵

46. Na vyovyote vile, tukikuonyesha baadhi ya tunayo waahidi, au tukakufisha kabla yake, marejeo yao ni kwetu. Kisha Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa wanayo yafanya.⁴⁶

47. Na kila umma una Mtume. Alipo wajia Mtume wao walihukumiwa baina yao kwa uadilifu, wala hawakudhumiwa.⁴⁷

48. Na wanasema: Lini ahadi hii, ikiwa mnasema kweli?⁴⁸

49. Sema: Sijimilikii nafsi yangu shari wala kheri ila apendavyo Mwenyezi Mungu. Kila umma una muda wao walio wekewa. Ukifika muda wao hawakawii hata saa moja

41 Na ewe Mtume! Wakishikilia kuendelea na kukukadhibisha baada ya kuwadhihirikia wazi dalili za Unabii wako, basi wewe waambie: Hakika mimi nitalipwa kwa a'mali yangu, (vitendo vyangu); na nyinyi mtalipwa kwa a'mali yenu kama itakavyo kuwa. Na mimi naendelea na Wito wangu, na nyinyi hamtahasabiwa kwa a'mali yangu, wala mimi sitahisabiwa kwa a'mali yenu. Basi nyinyi fanyeni mpendavyo. Na Mwenyezi Mungu atamlipa kila mtu kwa aliyo yachuma.

42 Na katika hawa makafiri wapo wanao kusikiliza wewe, Mtume, pale unapo waita wafuate Dini ya Mwenyezi Mungu, na hali nyoyo zao zimefungwa hazikubali Wito wako. Basi wewe huwezi kuwafanya hawa viziwi wakusikie na waongoke. Na khasa ilivyo kuwa juu ya uziwi wao, hawafahamu uyasemayo.

43 Na wengine wapo wanao kutazama na wanalifikiria jambo lako, na wanaona dalili zilizo wazi za Unabii wako. Lakini bado hawaongoki wakafuata. Mfano wa hayo ni mfano wa kipofu, nawe huwezi kuwaongoa hao vipofu. Upofu wa macho ni kama upofu wa moyo. Wote hawana uwongofu! Kipofu haioni njia kwa kuhisi, na mpotovu haongoki kwa maana.

44 Hakika Mwenyezi Mungu *Subhanahu* atawalipa watu kwa vitendo vyao kwa uadilifu na haki, wala hatamdulumu hata mmoja wapo kwa kitu chochote. Lakini watu wanajidhulumu nafsi zao kwa kukhiari kwao ukafiri kuliko Imani.

45 Ewe Mtume! Wahadharishe na Siku tutayo wakusanya kwa ajili ya Hisabu, wawe na hakika kuwa Siku ya Akhera itakuja, baada ya kuwa walikuwa wakiikanusha na wakikumbuka maisha yao ya duniani tu. Waone ni kama saa moja tu ya mchana, hapana wasaa wa kufanya kitendo chochote cha kheri, na wajuane wao kwa wao wakilaumiana kwa kufuru na upotovu walio kuwa nao! Wamekhasiri wakanushao Siku ya Akhera na wasitangulize vitendo vyema katika dunia yao, na wakakosa neema za Akhera kwa kufuru zao.

46 Ewe Mtume! Tukikuonyesha baadhi ya tunayo waahidi, nayo kuwa utawashinda na wao watapata adhabu, au tukakufisha kabla ya kuyaona yote hayo, vyovyote vile hawawezi kuepuka kurejea kwetu tuwahisabie na kuwalipa. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni Mwenye kuwachungua na Mwenye kujua kila walitendalo, naye atawalipa.

47 Na kila umma ulijiwa na Mtume akafikisha wito wa Mwenyezi Mungu, akaamini aliye amini, na akakanusha aliye kanusha. Ikifika Siku ya kufufuliwa, Mtume wao atakuja na kuwatolea ushahidi wale walio mkadhibisha kuwa hao ni makafiri, na walio amini kuwa ni Waumini. Basi Mwenyezi Mungu atawahukumu kwa uadilifu ulio timia. Hatomdhulumu yeyote katika malipo anayo stahiki.

48 Na makafiri wanakusudia kuikanusha Siku ya Akhera, basi wanaihimiza kwa kejeli na kusema: Itakuwa lini hiyo adhabu unayo tuahidi, kama wewe, ewe Mtume, na hao walio pamoja nawe, ni wakweli katika hayo mnayo yaamini na mnatuitia sisi tuyakubali?

wala hawatangulii.⁴⁹

50. Sema: Mwaonaje ikikufikieni hiyo adhabu yake usiku au mchana, sehemu gani ya adhabu wanaihimiza wakosefu?⁵⁰

51. Tena je! Ikisha tokea mtaiamini? Je! Ndio sasa tena? Na nyinyi mlikuwa mkiihimiza.⁵¹

52. Kisha walio dhulumu wataambiwa: Onjeni adhabu ya kudumu. Kwani mtalipwa isipo kuwa yale mliyo kuwa mkiyachuma?⁵²

53. Na wanakuuliza: Je! Ni kweli hayo? Sema: Ehe! Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hakika hayo ni kweli, na wala nyinyi hamshindi!⁵³

54. Na lau kuwa kila nafsi iliyo dhulumu inamiliki kila kiliomo duniani, bila ya shaka ingeli toa vyote kujikombolea. Na watakapo iona adhabu wataficha majuto. Na patahukumiwa baina yao kwa uadilifu, nao hawatadhulumuwa.⁵⁴

55. Jueni kuwa hakika vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi ni vya Mwenyezi Mungu. Jueni kuwa hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya haki. Lakini wengi wao hawajui.⁵⁵

56. Yeye ndiye anaye fufua na anaye fisha. Na kwake mtarejeshwa.⁵⁶

57. Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na poza kuponyesha yaliyomo vifuani, na uwongofu, na rehema kwa Waumini.⁵⁷

49 Ewe Mtume! Waambie: Mimi sina uwezo wa kujitendea mwenyewe kheri wala shari, ila kwa aliyo niwezesha Mwenyezi Mungu. Basi vipi niweze kuihimiza ije upesi hiyo adhabu? Hakika kila umma una ukomo wake aliyo uwekea Mwenyezi Mungu tangu na tangu. Ukiwadia ukomo huo basi hawatoweza kuuchelewesha hata kidogo, kama wasivyo weza kuutanguliza!

50 Waambie wanao himiza ifike adhabu: Hebu niambieni, ikikufikieni adhabu ya Mwenyezi Mungu usiku au mchana, pana faida gani watayo ipata wakosefu wenye madhambi kutaka ije kwa haraka? Na hali adhabu yote ni mbaya!

51 Sasa mnaikanusha adhabu? Tena itapo kufikieni mtaambiwa kwa kubeuliwa: Je! Sasa mnaamini kwa kuwa mnaiona, na nyinyi huko duniani mlikuwa mkiihimiza kwa dharau na kukanusha!

52 Tena Siku ya Kiama wataambiwa walio jidhulumu nafsi zao kwa kukufuru na kukanusha: Onjeni adhabu ya milele...sasa hamlipwi ila kwa a'mali zenu mlizo zitenda duniani.

53 Na makafiri, kwa njia ya kejeli na kukataa, wanakutaka wewe, Mtume, uwaambie hivyo ni kweli hayo uliyo yaleta katika Qur'ani na khabari za kufufuliwa, na adhabu? Waambie: Naam! Kwa haki ya Muumba wangu aliye numba, hakika hayo yatakuwa bila ya shaka yoyote. Wala nyinyi hamtoshinda wala hamwezi kuzuia adhabu aitakayo Mwenyezi Mungu kukuleteeni.

54 Na lau kuwa vitu vyote viliomo duniani ni mali ya kila nafsi iliyo dhulumu kwa ushirikina na kukanusha, ingeli vitoa fidia kwa adhabu itayo wakabili Siku ya Kiyama, na ambayo wataviona vitisho vyake. Na hapo basi majuto na masikitiko yatawajaa nyoyoni mwao kwa kutoweza kuyatamka, na kwa fazaa itayo wapata kwa kuiona adhabu! Na hukumu ya Mwenyezi Mungu itapita juu yao kwa uadilifu, na wala hawatodhulumuwa katika malipo hayo, kwani hayo ni matokeo ya waliyo yatenda duniani!

55 Watu nawajue kuwa hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kumiliki na Mwenye madaraka makuu juu ya vyote viliomo mbinguni na duniani. Na pia wajue kuwa ahadi yake ni ya kweli. Basi Yeye hashindwi na kitu, na hapana yeyote ataye epuka malipwa yake. Lakini wao wamedanganyika na maisha ya dunia, hawajui hayo kwa ujuzi wa yakini!

56 Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* anavihuisha vitu baada ya kuwa havipo, na anaviiondoa baada ya kuwapo. Na kwake Yeye tu ndio marejeo katika Akhera. Na mwenye kuwa hivyo hapana kuu la kumshinda.

57 Enyi watu! Kimekujieni kwa ulimi wa Mtume Muhammad Kitabu kilicho toka kwa Mwenyezi Mungu. Ndani yake mna makumbusho ya Imani, na ut'iifu, na mawaidha ya kuhimiza kheri, na kukataza vitendo viovu, na kueleza mzingatie khabari za walio kutangulieni, na kukutakeni muangalie utukufu wa umbaji ili mpate kuelewa utukufu wa Muumba. Na ndani ya Kitabu hicho mna dawa ya maradhi ya nyoyo zenu, maradhi ya shiriki na unaafiki; na mna uwongofu wa kuendea Njia Iliyo Nyooka. Na yote hayo ni rehema kwa Waumini wanao itikia wito.

- 58.** Sema: Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema yake! Basi nawafurahi kwa hayo. Haya ni bora kuliko hayo wanayo yakusanya.⁵⁸
- 59.** Sema: Je! Mwaonaje zile riziki alizo kuteremshieni Mwenyezi Mungu, nanyi mkafanya katika hizo nyengine haramu na nyengine halali. Sema: Je! Mwenyezi Mungu amekuruhusuni, au mnamzulia Mwenyezi Mungu tu?⁵⁹
- 60.** Na nini dhana ya wanao mzulia Mwenyezi Mungu kwa Siku ya Kiyama? Hakika Mwenyezi Mungu ana fadhila juu ya watu, lakini wengi wao hawashukuru.⁶⁰
- 61.** Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur'ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilicho wazi.⁶¹
- 62.** Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika.⁶²
- 63.** Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu.⁶³
- 64.** Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hapana mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu. Huko ndiko kufuzu kukubwa.⁶⁴
- 65.** Wala yasikuhuzunishe maneno yao. Hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua.⁶⁵

58 Ewe Mtume! Waambie: Furahieni fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema yake juu yenu kwa kuiteramsha Qur'ani, na kubainisha Sharia ya Islamu. Na hii ni bora kuliko starehe zote anazo zikusanya mtu duniani, kwa sababu hichi ni chakula cha nyoyo na dawa ya maradhi yake.

59 Ewe Mtume! Waambie makafiri walio pewa baadhi ya starehe za duniani: Niambieni khabari ya vyakula vizuri vya halali alivyo kuruzukuni Mwenyezi Mungu, mkajifanya wenyewe ni watungaji sharia, mkahalalisha vingine na mkaharimisha vingine, bila ya kufuata Sharia ya Mwenyezi Mungu! Hakika Mwenyezi Mungu hakukupeni ruhusa mfanye hayo, bali nyinyi mnamzulia uwongo Mwenyezi Mungu.

60 Na watadhani nini Siku ya Kiyama hao walio mzulia uwongo Mwenyezi Mungu, wakajipa kuhalalisha na kuharimisha bila ya kuwa nayo dalili yoyote? Hakika Mwenyezi Mungu amewaneemesha neema nyingi na amezihalalisha kwao kwa fadhila yake, na amewawekea Sharia yenye kheri kwao. Lakini hawamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hayo, bali wanamzulia Mwenyezi Mungu uwongo!

61 Ewe Mtume! Hakika wewe umefikisha ujumbe wako, na hayo Mwenyezi Mungu anayajua. Na hapana jambo lolote katika mambo yako, na huwasomei Qur'ani, na wewe na umma wako hamtendi kitu, ila Sisi tunayashuhudia na tunayaangalia mnapo yaingia kwa juhudi. Na Mola wako Mlezi haachi kujua chochote hata kikiwa kina uzito wa chembe hichi, ikiwa katika mbingu au katika ardhi, kidogo na kikubwa. Vyote hivyo vinadhibitiwa katika Kitabu kilichoko kwa Mwenyezi Mungu, nacho ni chenye kubainisha wazi.

62 Enyi watu! Tanabahini na mjue ya kuwa wenye kumuelekea Mwenyezi Mungu kwa Imani na ut'iifu Yeye anawapenda, na wao wanampenda. Hawana khofu ya kuhizika duniani, wala kupata adhabu ya Akhera. Wala wao hawahuzuniki kwa kukosa starehe za duniani, kwa kuwa watapata kwa Mwenyezi Mungu yaliyo makubwa na mengi kuliko hayo.

63 Na hao ndio walio yasadiki yote yaliyo toka kwa Mwenyezi Mungu, na wakaifuata Haki, na wakayaepuka maasi, na wakamkhofu Mwenyezi Mungu katika kila walitendalo.

64 Kwa wapenzi hawa wa Mwenyezi Mungu pana bishara ya kheri hapa duniani, kwa vile Mwenyezi Mungu amewaahidi kuwapa ushindi na utukufu, na Akhera itatimia ahadi ya Mwenyezi Mungu. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu haigeuki. Na haya ndiyo waliyo bashiriwa kwayo duniani, na watayapata Akhera. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.

65 Ewe Mtume! Usihuzunuke kwa wayasemayo washirikina ya kejeli, na matusi, na kukadhibisha. Wala usidhani kuwa hali yao hii itadumu. Bali ushindi ni wako, na Uislamu utatukuka, kwani utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ushindi upo mkononi mwake, na Yeye atakunusuru uwashinde hao makafiri. Na Yeye *Subhanahu* ni Mwenye kuyasikia wanayo kuzulia, na Mwenye kuyajua wanayo dhamiria. Na Yeye atawalipa kwa hayo.

66. Jueni kuwa ni vya Mwenyezi Mungu vyote viliomo mbinguni na ardhinii. Na wala hawawafuati hao wanao waomba badala ya Mwenyezi Mungu kuwa ni washirika wake. Wao hawafuati ila dhana tu, na hawasemi ila uwongo.⁶⁶

67. Yeye ndiye aliye kujaalieni usiku mpate kutulia humo, na mchana wa kuonea. Hakika katika haya zipo Ishara kwa watu wanao sikia.⁶⁷

68. Wamesema: Mwenyezi Mungu ana mwana. *Subhanahu*, Aliye takasika! Yeye ni Mkwasi, Mwenye Kujitosheleza. Vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi ni vyake peke yake. Nyinyi hamna uthibitisho wowote wa haya! Mnamzulia Mwenyezi Mungu msiyo yajua?⁶⁸

69. Sema: Hao wanao mzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa.⁶⁹

70. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo yao ni kwetu. Tena tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.⁷⁰

71. Wasomee khabari za Nuhu alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu nanyi na kukumbusha kwangu kwa Ishara za Mwenyezi Mungu kunakutieni mashaka basi mimi namtegemea Mwenyezi Mungu. Nanyi tengezeni mambo yenu pamoja na washirika wenu, na wala mambo yenu yasifichikane kwenu. Kisha nihukumuni, wala msinipe muhula.⁷¹

72. Lakini mkigeuka, basi mimi sikukuombeni ujira. Ujira wangu hauko ila kwa Mwenyezi Mungu. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu.⁷²

66 Enyi watu! Jueni kuwa ni vya Mwenyezi Mungu peke yake vyote viliomo mbinguni na duniani, kwa kuviumba, na kuvimiliki, na kuviendesha. Na hao wanao mshirikisha Mwenyezi Mungu kwa hakika hawawafuati hao miungu ya ushirikina. Hao si chochote ila wanafuata mawazo tu, wanadhani kuwa uwezo umo katika vitu ambavyo havijifai wenyewe, la kwa manufaa wala madhara.

67 Hakika huyo Mwenyezi Mungu kumiliki viliomo katika mbingu na ardhi, ndiye aliye kuumbieni usiku mpate kupumzika na mahangaiko ya mchana. Na amekuumbieni mchana wenye kuangaza mpate kufanya kazi na mshughulikie maslaha yenu. Hakika katika kuumbwa usiku na mchana zipo dalili zilizo wazi kwa wenye kusikia na wakapima.

68 Na ikiwa wanao abudu masanamu wamefanya ushirikina wa kuabudu mawe, na hawakumtakasa Mwenyezi Mungu kwa haki ya kumtakasa, na wakasema kuwa Allah, Mwenyezi Mungu, ana mwana, basi Mwenyezi Mungu ametakasika na hayo. Yeye hana haja ya kuwa na mwana; kwani kuwa na mwana kunaonyesha wazi kutaka kubakia ukoo wako baada ya kufa kwako. Na Mwenyezi Mungu hafi. Yeye ni Mwenye kubakia milele. Na vyote viliomo katika mbingu na viliomo katika ardhi ni vyake, vimeumbwa na vinaendeshwa na Yeye. Na nyinyi wazushi, hamna hoja yoyote wala dalili ya hayo mnayo zua! Basi msikhitalifiane juu ya Mwenyezi Mungu kwa mambo yasiyo na msingi wa hakika.

69 Ewe Mtume! Waambie: Hao wanao mtungia Mwenyezi Mungu uwongo, na wanadai kuwa ana mwana, hawatafanikiwa milele.

70 Wao wana starehe hapa duniani ya kudanganyika nayo. Nayo ni chache, ikiwa itachukua muda mrefu au mfupi, ukilinganisha na hayo yanayo wangojea! Kisha marejeo yao ni kwetu, Sisi. Tutawahisabia na tutawaonjesha adhabu ya kutia uchungu kwa sababu ya ukafiri wao.

71 Yanayo kupata kutoka kwa watu wako, yaliwapata Manabii walio kutangulia. Basi wasomee hawa watu, Ewe Mtume, aliyo kuteremshia Mola wako Mlezi katika Qur'ani kisa cha Nuhu, Mtume wa Mwenyezi Mungu. Alipo iona chuki na uadui wa watu wake kwa ujumbe wake, aliwaambia: Enyi watu wangu! Ikiwa kuwa pamoja nanyi kwa ajili ya kufikisha ujumbe kumekuwa ni shida juu yenu, basi mimi ni mwenye kuendelea na wito wangu, na ni mwenye kushikilia hapo hapo, na ni mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu katika hili jambo langu. Basi nyinyi na washirika wenu jifungeni madhubuti katika shauri yenu, wala msifuche uadui wenu kwangu kabisa, wala msinipe muhula wowote kwa maovu mnayo nipangia kunitendea, kama kweli mnaweza kunitelea madhara. Kwani Mola wangu Mlezi ananilinda.

72 Na ikiwa mtabaki kukataa wito wangu, basi hayo hayatanidhuru mimi kitu. Kwani mimi sikufanya hivyo kwa kutaraji kupokea ujira kwenu ambao naogopa nitaukosa, kwa sababu ya kukataa kwenu! Ujira wangu mimi nautaka kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Na Yeye ameniamrisha niwe Muislamu,

- 73.** Wakamkanusha. Basi tukamwokoa, pamoja na walio kuwa naye, katika jahazi. Na tukawafanya wao ndio walio bakia, na tukawazamisha walio zikanusha Ishara zetu. Basi angalia vipi ulikuwa mwisho wa walio onywa.⁷³
- 74.** Kisha baada yake tukawatuma Mitume kwa watu wao. Nao wakawajia kwa Ishara zilizo wazi. Lakini hawakuwa wenye kuyaamini waliyo yakanusha kabla yake. Ndio kama hivyo tunapiga muhuri juu ya nyoyo za warukao mipaka.⁷⁴
- 75.** Kisha baada yao tukamtuma Musa na Haruni kwa Firauni na waheshimiwa wake, kwa Ishara zetu. Wakajivuna, na wakawa watu wakosefu.⁷⁵
- 76.** Basi ilipo wajia Haki kutoka kwetu walisema: Hakika huu ni uchawi dhaahiri.⁷⁶
- 77.** Akasema Musa: Mnasema hivi juu ya Haki ilipo kujieni? Huu ni uchawi? Na wachawi hawafanikiwi!⁷⁷
- 78.** Wakasema: Je! Umetujia ili utuachishe tuliyo wakuta nayo baba zetu, na mpate nyinyi wawili ukubwa katika nchi? Wala sisi hatukuaminini nyinyi.⁷⁸
- 79.** Na Firauni akasema: Nileteeni kila mchawi mjuzi!⁷⁹
- 80.** Basi walipo kuja wachawi, Musa aliwaambia: Tupeni mnavyo tupa!⁸⁰
- 81.** Walipo tupa, Musa alisema: Mliyo leta ni uchawi. Hakika Mwenyezi Mungu haitengenezi kazi ya waharibifu.⁸¹

nimsalimishie Yeye mambo yangu yote.

73 Na juu ya juhudi hizo, na kukakamia huko aliko kakamia Nuhu kwa ajili ya kutaka kuwaongoa hao watu wake, bado walishikilia kuendelea na kumkanusha na kumfanyia uadui. Basi Mwenyezi Mungu alimwokoa yeye pamoja na wenye kumuamini, wakapanda marikebu. Na akawajaalia hao ndio walio iamirisha nchi baada ya kuteketea makafiri, walio gharikishwa na tofani. Hebu angalia, ewe Muhammad! Vipil walio puuza onyo ulivyo malizikia mwisho wao mbaya.

74 Baada ya Nuhu tuliwatuma Mitume wengine wakilingania Tawhid, Upweke wa Mwenyezi Mungu, wakibashiria kheri na wakionya, na wakiungwa mkono na miujiza yenye kuonyesha ukweli wao. Watu wao wakawakanya kama walivyo kanya kaumu ya Nuhu. Haukuwa mwendo wa wapinzani kuwa wat'ifu, kwa sababu kule kukadhbisha kwao kulikuwa ni mbele kuliko kuzingatia na kupima. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu alipiga muhuri wa upotovu juu ya nyoyo za wale ambao mtindo wao ni kuzifanyia uadui hakika na Ishara zilizo wazi!

75 Kisha baada yao tulimtumia Musa na ndugu yake Haruni wende kwa Firauni, mfalme wa Misri na watu wake wakuu makhsusi, kuwaita wamuabudu Mwenyezi Mungu peke yake. Nao waliungwa mkono na hoja zenye nguvu. Firauni na kaumu yake walitakabari wakakataa kuitikia wito wa Musa na Haruni. Kwa kukataa kwao huko wakawa wamefanya makosa makubwa na dhambi.

76 Ilipo dhihiri Haki yetu kwa mkono wa Musa, ule muujiza wa Musa - nao ni fimbo kugeuka nyoka mbele ya macho yao - wao walisema: Hakika huu ni uchawi ulio dhaahir!

77 Musa akawaambia kukanya uzushi wao: Nyinyi mnaita Haki iliyo toka kwa Mwenyezi Mungu kuwa ni uchawi? Hivyo hii kweli mliyo iona kwa macho yenu ni uchawi? Basi hivi hapa mimi nakutakeni mthibitishie kwamba huu ni uchawi. Waleteni wachawi wathibitishie hayo mnayo yadai. Na wachawi hawafanikiwi abadan!

78 Firauni na watu wake walimwambia Musa: Hapana shaka wewe umekuja kwa makusudi ya kutuachisha dini ya baba zetu, na mila za kaumu yetu, ili nyinyi wawili mpate kuwa na wafuasi; wewe na nduguyo mpate ufalme na utukufu na urais wa kutawala na kuhukumu! Kwa hivyo basi sisi hatutakuaminini nyinyi wala huo utume wenu!

79 Firauni na kaumu yake wakadai kuwa Musa na nduguye ni wachawi, wala si Mitume! Akawataka watu wake wamhudhurishe kila aliye hodari katika fani za uchawi katika mamlaka yake.

80 Walipo hudhuria wachawi, na wakasimama mbele ya Musa kupambana naye kwa uchawi wao mbele ya watu, Musa aliwaambia: Leteni huo uchawi mlilo nao!

81 Walipo tupa kamba zao na fimbo zao, Musa aliwaambia: Huo mlilo fanya ni uchawi kweli, na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* atauvunja kwa mkono wangu! Hakika Mwenyezi Mungu hawasahilishii mafisadi vitendo vyao vikawa vizuri na vyenye nafuu.

- 82.** Na Mwenyezi Mungu huhakikisha Haki kwa maneno yake, hata wanga chukia wakosefu.⁸²
- 83.** Basi hawakumuamini Musa isipo kuwa baadhi ya vijana vya kaumu yake, kwa kumwogopa Firauni na wakuu wao wasiwatase. Kwani hakika Firauni alikuwa jeuri katika nchi. Na kwa yakini alikuwa miongoni mwa walio pita kiasi.⁸³
- 84.** Na Musa alisema: Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu.⁸⁴
- 85.** Wakasema: Tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Ewe Mola wetu Mlezi! Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na hao watu madhaalimu.⁸⁵
- 86.** Na utuokoe kwa rehema yako na watu makafiri.⁸⁶
- 87.** Na tukampelekea Musa na ndugu yake wahyi huu: Watengenezeeni majumba watu wenu katika Misri na zifanyeni nyumba zenu ndio mwahali mwa ibada, na mshike Sala, na wabashirie Waumini.⁸⁷
- 88.** Na Musa akasema: Mola wetu Mlezi! Hakika wewe umempa Firauni na wakuu wake mapambo na mali katika maisha ya dunia. Hivyo wanapoteza watu na Njia yako. Mola wetu Mlezi! Yafutilie mbali mali yao na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu.⁸⁸
- 89.** Mwenyezi Mungu akasema: Maombi yenu yamekubaliwa. Basi simameni sawa sawa, wala msifuate njia za wale wasio jua.⁸⁹
- 90.** Tukawavusha bahari Wana wa Israili, na Firauni na askari wake wakawafuatia kwa dhulma na uadui. Hata Firauni alipo kuwa anataka kuzama akasema: Naamini kuwa hapana mungu ila yule waliye muamini Wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa walio nyenyekea!⁹⁰

82 Ama Haki hapana shaka Mwenyezi Mungu atainusuru na ataiunga mkono kwa uwezo wake na hikima yake hata makafiri wakisaidiana katika kuichukia na kuipiga vita.

83 Na juu ya kudhihiri Ishara zote za kusadikisha Ujumbe, wale walio muamini Musa hawakuwa ila ni kikundi cha watu wachache tu katika kaumu ya Firauni. Waliamini juu ya kuwa wakiogopa asije Firauni na walio pamoja naye wakawaachisha waliyo yaamini. Jeuri za Firauni zilikuwa kubwa mno katika Misri! Hakika yeye ni katika walio pita upeo katika kutakabari na kujivuna.

84 Ama Musa aliwaambia Waumini kwa kuwawasa na kuwashajiisha: Enyi watu wangu! Ikiwa Imani imekwisha ingia nyoyoni mwenu kwa kumsafishia niya Mwenyezi Mungu, basi msimwogope yeyote mwengine. Nanyi msalimishie Yeye mambo yenu yote, na mtegemeeni Yeye, na muwe na yakini mwishoe atakunusuruni, ikiwa nyinyi mmethibiti katika Uislamu.

85 Waumini wakasema: Tunamtegemea Mwenyezi Mungu peke yake. Kisha wakamwomba Mola wao Mlezi asiwatie katika mitihani na mateso ya makafiri.

86 Wakamwomba Mola wao Mlezi wakisema: Kwa vile ulivyo tumiminia neema na rehema, na kwa wingi wa rehema yako unayo sifika nayo, tuokoe na hawa watu wanao kataa, wenye kudhulumu.

87 Tukawafunulia Musa na nduguye Haruni kuwapa amri wafanye nyumba za kukaa watu wao katika nchi ya Misri, na watu wa Imani wenye kufuata wito wa Mwenyezi Mungu wazielekee nyumba hizo, na wawe wanashika Sala kwa sura ya ukamilifu. Na Waumini wanabashiriwa kheri!

88 Walivyo shikilia makafiri katika kumfanyia inda Musa, alimwomba Mwenyezi Mungu kwa kusema: Ewe Mola Mlezi wangu! Hakika Wewe umempa Firauni na watukufu wake starehe za duniani, na mali, na wana, na utawala. Na matokeo ya neema hizi ni kupita kwao mipaka katika kupotea na kupoteza watu waache Njia ya Haki! Ewe Mwenyezi Mungu! Yafutilie mbali mali yao, na uwaache katika kiza cha nyoyo zao, wasijaaliwe kuipata Imani mpaka waione kwa macho adhabu iliyo chungu, ambayo ndiyo mwisho unao wangojea, ili wawe ni onyo kwa wengineo.

89 Mwenyezi Mungu akasema: Dua zenu zimeitikiwa. Basi endeleeni katika Njia Iliyo Nyooka, na iwacheni njia ya wale wasio jua mambo yalivyo, wala hawaifuati Haki iliyo wazi.

90 Tulipo wavusha bahari Wana wa Israili, Firauni na askari wake waliwafuatia nyuma yao, tukawafunika

91. Ala! Sasa? Na hali uliasi kabla yake na ukawa miongoni mwa mafisadi!⁹¹
92. Leo, basi, tutakuokoa kwa mwili wako, ili uwe Ishara kwa ajili ya walio nyuma yako. Na hakika watu wengi wameghafilika na Ishara zetu.⁹²
93. Na hakika tuliwaweka Wana wa Is raili kikao chema, na tukawaruzuku vitu vizuri. Nao hawakuhitalifiana mpaka ilipo wafikia ilimu. Hakika Mola wako Mlezi atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyo kuwa wakikhitalifiana.⁹³
94. Na ikiwa unayo shaka katika tuliyo kuteremshia, basi waulize wasomao Kitabu kabla yako. Kwa yakini imekwisha kujia Haki kutoka kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wenye shaka.⁹⁴
95. Na kabisa usiwe miongoni mwa wale wanao zikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, usije kuwa katika walio khasiri.⁹⁵
96. Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini,⁹⁶
97. Ijapo kuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu.⁹⁷
98. Kwa nini usiwepo mji mmoja ukaamini na Imani yake ikawafaa - isipo kuwa kaumu Yunus? Waliamini na Sisi tukawaondolea adhabu ya hizaya katika maisha ya dunia, na tukawastarehesha kwa muda.⁹⁸
99. Angeli taka Mola wako Mlezi wangeliki amini wote waliomo katika ardhi. Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?⁹⁹

kwa bahari! Alipo kuwa anazama, Firauni alisema: Nimemsadiki Allah, Mwenyezi Mungu, walio msadiki Wana wa Israili, na wakamfuata. Na mimi ni katika wenye kut'ii walio wanyenyekevu.

91 Mwenyezi Mungu hakukupokea kuamini huko kwa Firauni ambako alikuwa hana budi nako. Toba hiyo ilikuwa pale mauti yamekwisha mkabili, naye aliishi maisha yake yote katika kumuasi Mwenyezi Mungu, akifisidi nchi, naye akafa kafiri wa kutupwa!

92 Na leo siku ulipo angamia tutaotoa mwili wako baharini, na tutauweka uwe ni onyo na funzo kwa hao walio kuwa wakikuabudu, na hawakuwa wakikutarajia utapata mwisho huu wa hizaya wa machungu. Lakini watu wengi wanaghafilika na Ishara zilizo wazi na zilizo zagaa katika ulimwengu, na ambazo zinathibitisha uwezo wetu. (*Tazama Maelezo 10:92*)

93 Na tuliwaweka vyema Wana wa Israili wakaishi katika nchi nzuri na huku wakiifadhi Dini yao, nao wako mbali na dhulma iliyo kuwa ikiwapata; riziki na neema zimewajalia. Lakini mara baada ya kuonja neema ya utukufu baada ya unyonge, yaliwasibu maradhi ya kufarikiana. Wakakhitalifiana juu ya kuwa imekwisha bainika kweli na uwongo! Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao Siku ya Kiyama, na atamlipa kila mmoja kwa alilo tenda.

94 Ikikuingia shaka wewe au mwengineo katika huu wahyi tuliyo kuteremshia, basi waulize watu wa Vitabu vilivyo tangulia walivyo teremshiwa Manabii wao. Kwao utapata jawabu ya kukata, yenye kuwafikiana na haya tuliyo kuteremshia wewe. Na hayo ni kutilia mkazo ukweli wa uwazi wa dalili pindi ikitokea shaka yoyote. Basi hapana njia ya kutia shaka. Sisi tumekuteremshia Haki isiyo na shaka yoyote. Basi usishindane na yeyote mwengineo katika kutia shaka na kutaradadi.

95 Wala usiwe wewe, wala yeyote katika wanao kufuata, miongoni mwa wanao kadhibisha hoja na Ishara zilizo wazi, msije mkaingia khasarani na ghadhabuni, kama hali ya makafiri wasio amini. Na akisemezwa Nabii basi ndio wanasemezwa wote wanao mfuata.

96 Hakika wale iliyo kwisha pita juu yao hukumu ya kuwa wao ni makafiri, kwa kujulikana inadi yao na chuki zao, hawataamini hata ukijihangaisha vipi nafsi yako kuwakinaisha.

97 Na ukiwajia na kila hoja, na iwe wazi vipi, hawakinaiki. Wataendelea tu na upotovu wao mpaka wamalizikie kupata adhabu chungu.

98 Lau kila mji ungeli amini ingeli wafaa Imani yao. Lakini hawaamini, na kwa hivyo hayapatikani manufaa. Ila kaumu ya Yunus. Kwani wao waliamini, na wakapata manufaa yao. Tuliwaondolea hizaya na machungu, na tukawapa starehe ya dunia inayo pita, mpaka ifike Siku ya Kiyama.

99 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka watu wote katika ardhi waamini, wangeliki amini. Basi wewe usihuzunike kwa ukafiri wa washirikina. Wala haiwi Imani ila kwa khiari. Basi wewe huwezi

100. Na hawezi mtu kuamini ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Naye hujaalia adhabu iwafike wasio tumia akili zao.¹⁰⁰

101. Sema: Angalieni yaliomo mbinguni na kwenye ardhi! Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasio amini.¹⁰¹

102. Basi, je! Wanangojea jingine ila kama yaliyo tokea siku za watu walio pita kabla yao? Ngojeni! Nami ni pamoja nanyi katika wanao ngoja.¹⁰²

103. Kisha Sisi huwaokoa Mitume wetu na walio amini. Ndio kama hivyo, inatustahiki kuwaokoa Waumini.¹⁰³

104. Sema: Enyi watu! Ikiwa nyinyi mnayo shaka katika Dini yangu, basi mimi siwaabudu mnao waabudu nyinyi badala ya Mwenyezi Mungu. Lakini mimi namuabudu Mwenyezi Mungu anaye kufisheni. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waumini.¹⁰⁴

105. Na uelekeze uso wako kwenye Dini ya Kweli, wala usiwe katika washirikina.¹⁰⁵

106. Na wala usiwaombe wasio kuwa Mwenyezi Mungu ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru. Ukifanya hivyo basi utakuwa miongoni mwa walio dhulumu.¹⁰⁶

107. Na Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake. Huifikisha kwa amtakaye katika waja wake, na Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.¹⁰⁷

108. Sema: Enyi watu! Haki imekwisha kukujieni kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Basi anaye ongoka anaongoka kwa faida ya nafsi yake, na anaye potea anapotea kwa

kuwalazimisha watu kwa nguvu ili wafuate Haki na waitikie. Haikupasii kutaka kuwalazimisha waamini, wala hutoweza, hata ukijitahidi vipi.

100 Hawezi mtu kuamini ila akiielekeza nafsi yake kwa hayo, na Mwenyezi Mungu akamsahilishia sababu na njia za hayo. Ama yule asiye ielekea Imani huyo basi amestahiki kukasirikiwa na Mwenyezi Mungu, na kupata adhabu yake. Na mwendo wa Mwenyezi Mungu ni kuwapa adhabu na ghadhabu wale wanao zipuza na kuzikataa hoja zilizo wazi, na wala hawazizingatii.

101 Ewe Nabii! Waambie hawa wenye inda: Tazameni Ishara zilizo wazi zinazo onyesha Ungu na Upweke wa Mwenyezi Mungu zilizo enea katika mbingu na ardhi. Lakini Ishara, juu ya wingi wake, na maonyo na yangawa na nguvu, hayawafai kitu watu wanao kataa na wala hawatunii akili zao. Hawa wanao kanya kama hawaamini, basi hawatoangalia. (*Tazama Maelezo 10:101*)

102 Basi hao wakanyao wanangojea lolote ila kufikiwa na siku za shida kama zilizo wapata kaumu ya Nuhu, na kaumu ya Musa, na wengineo? Ewe Nabii! Waambie: Ikiwa mnangojea mfano wa hayo, basi ngojeni! Nami pia nangojea pamoja nanyi. Na karibu hivi mtasibiwa na kushindwa, na Siku ya Kiyama mtapata adhabu.

103 Kisha Sisi huwaokoa Mitume wetu na Waumini kutokana na adhabu hiyo. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amewaahidi kuwaokoa, na ahadi yake ni ya kweli, wala hayendi kinyume.

104 Ewe Mtume! Waambie: Ikiwa mna shaka na ukweli wa Dini niliyo tumwa kuileta kwenu, basi jueni kuwa kama mtavyo tia shaka mimi kabisa sitoabudu hayo masanamu mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu! Lakini mimi namuabudu Mwenyezi Mungu ambaye mambo yenu yote yapo mikononi mwake. Yeye ndiye anaye kutoeni roho. Na Yeye ameniamrisha niwe katika wanao muamini Yeye.

105 Ewe Nabii! Simama sawasawa, umuelekee Mwenyezi Mungu vilivyo. Wala usijitie katika miongoni mwa walio mshirikisha Mwenyezi Mungu. Epukana nao, na uwe mbali nao, wewe na Waumini wanao kufuata.

106 Wala usimkimbilie kwa kumwomba na kumuabudu yeyote asiye kuwa Mwenyezi Mungu. Hao hawakuletei manufaa wala madhara. Ukifanya hayo inakuwa umekwisha ingia miongoni mwa washirikina walio dhulumu. Na anayo katazwa Nabii, ndio wanakatazwa umma wake wote. Na hivyo ndio ukomo wa kukanya. Kwani kumkanya ambaye hayumkiniki kutenda anacho kanywa, ndio hadi ya kukanya.

107 Ewe Nabii! Yakikusibu madhara kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hapana wa kuyaondoa ila Yeye. Na akikujaalia kheri hapana anaye weza kukunyima yeyote. Kwani yeye anagawa kheri kuwapa waja wake kwa fadhila yake. Na Yeye *Subhanahu* ni Mkunjufu wa maghira, Mkuu wa rehema.

khasara ya nafsi yake. Na mimi si mwakilishi juu yenu.¹⁰⁸

109. Na wewe fuata yanayo funuliwa kwako kwa wahyi. Na vumilia mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu, na Yeye ndiye mbora wa mahakimu.¹⁰⁹

108 Ewe Mtume! Fikisha wito wa Mwenyezi Mungu kwa watu wote! Na waambie: Enyi watu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteremshieni Sharia ya Haki kutokana naye. Anaye taka kuongoka basi afanye haraka. Kwani faida ya uwongofu wake utamrejea mwenyewe. Na mwenye kushikilia upotovu utamuangukia mwenyewe. Na mimi sikuwakilishwa nikulazimisheni muamini, wala kukutawalini.

109 Ewe Mtume! Thibiti juu ya Dini ya Haki. Na fuata wahyi ulio teremshiwa, nawe uwe na subira kwa maudhi yanayo kufika kwa ajili ya Njia ya Da'wa (Wito), mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu baina yako na wao, kwa vile alivyo kuahidi kuwa atawapa ushindi Waumini, na watahizika makafiri. Na Yeye ndiye mbora wa mahakimu.

Sura 11 - Hud

Utangulizi

Surat Hud ni Sura ya Makka. Ina Aya 123. Imeanza kwa kuisifu Qur'ani Tukufu, na kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake, na kuonya, na kubashiria. Kisha ikabainisha uwezo wa Mwenyezi Mungu na kuwa Yeye ndiye Mola Mlezi. Na ikaeleza hali za watu katika kuzipokea kwao neema zake Mola Mlezi, na adhabu zake. Kisha ikataja cheo cha Qur'ani, na kufuru za makafiri bila ya udhuru wowote kwa ukafiri wao, na malipo ya Waumini.

Naye *Subhanahu* baada ya hayo amesimulia hadithi za Manabii, na majadiliano ya kaumu zao nao, na kuwateremkia makafiri adhabu ya duniani na kuokoka kwa Waumini. *Subhanahu wa Taa'la* akataja hadithi ya Nuhu kwa kupambanua zaidi kuliko ilivyo kuwa katika Surat Yunus. Humu imeelezwa fikra za kafiri na inadi yake, na imebainishwa ilivyo mteremkia chuki. Na baada ya hadithi ya Nuhu Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ametaja kisa cha A'ad pamoja na Nabii wa Mwenyezi Mungu Hud, kwa kueleza wazi mawazo ya ukafiri, na yaliyo wateremkia makafiri juu ya kuwa walikuwa na nguvu na wakali.

Kisha kikatajwa mfano wa hayo kisa cha Nabii wa Mwenyezi Mungu, Saleh pamoja na kabila la Thamud, na tena kisa cha *Nabiyyu Llah* na rafiki yake, Ibrahim. Kisha hadithi ya *Nabiyyu Llah*, Lut'. Kisha kisa cha *Nabiyyu Llah*, Shua'ib.

Kisha *Subhanahu wa Taala* ametaja nini mafunzo ya hadithi hizi za kweli, na akamalizia *Subhanahu* kwa kuwataka Waumini watende mema, na wangojee malipo. Tena ukatajwa ujuzi ulio kamilika wa Mwenyezi Mungu Aliye takasika na kutukuka, na waajibu wa kumtegemea Yeye.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Ra. Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimewekwa wazi, kisha zikapambanuliwa, kilicho toka kwa Mwenye Hikima na Mwenye Khabari,¹
2. Ili msimuabudu isipo kuwa Allah, Mwenyezi Mungu. Hakika mimi kwenu ni mwonyaji na mbashiri nitokae kwake.²
3. Na ili mumwombe msamaha Mola wenu Mlezi, kisha mtubie kwake. Atakustarehesheni starehe nzuri mpaka muda maalumu. Na atampa kila mwenye fadhila, fadhila yake. Na ikiwa mtakengeuka basi mimi nakukhofieni adhabu ya hiyo

1 Alif Lam Ra (A.L.R.). Hizi ni harufi zilizo anziwa Sura hii kuwa ni ishara kuwa Qur'ani ni muujiza juu ya kuwa imeundwa kwa hizi hizi harufi zinazo tamkwa, na pia ni kuwazindua watu wanapo isikiliza inapo somwa Qur'ani Tukufu kuwa ni Kitabu chenye shani kuu. Zimeteremshwa Aya zake zimeshikana, madhubuti, hazina ndani yake upotovu, wala ubabaishi, na zimetungwa kwa njia isiyo na dosari, iwazi, na yenye kubainisha. Kisha hukumu zake zikapambanuliwa. Na Kitabu hichi juu ya utukufu wake ulio nao nafsi yake, kina utukufu zaidi kwa kuwa kimetokana na Mwenyezi Mungu ambaye anajua kila kitu, na Yeye *Subhanahu* anapanga mambo yote kwa pahala pake.

2 Ewe Nabii! Waongoze watu kwa hii Qur'ani, na uwaambie: Msimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu tu. Na hakika mimi nimetumwa kutoka kwake ili nikuonyeni msikufuru ikakupateni adhabu yake, na nikupeni bishara njema kuwa mkiamini na mkat'ii, basi mtapata malipo yake.

Siku Kubwa.³

4. Marejeo yenu ni kwa Mwenyezi Mungu tu. Naye ni Muweza wa kila kitu.⁴

5. Hebu angalia! Ati wanafunika vilivyomo vifuani mwao ili wamfiche Mwenyezi Mungu! Jueni kuwa wanapo jigubika nguo zao Yeye anajua wanayo yaficha na wanayo yatangaza. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.⁵

6. NA HAKUNA mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.⁶

7. Na Yeye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Na Kiti chake cha Enzi kilikuwa juu ya maji, ili akufanyieni mtihani ajuulikane ni nani miongoni mwenu mzuri zaidi wa vitendo. Na wewe ukisema: Nyinyi hakika mtafufuliwa baada ya kufa; wale walio kufuru husema: Hayakuwa haya ila ni uchawi uliyo wazi.⁷

8. Na tukiwacheleweshea adhabu mpaka muda ulio kwisha hisabiwa wao husema: Nini kinacho izuia hiyo adhabu? Jueni! Siku itakapo wajia basi haitoondolewa hiyo kwao. Na yatawazunguka yale waliyo kuwa wakiyafanyia mzaha.⁸

9. Na tukimwonjesha mtu rehema inayo toka kwetu, kisha tukamwondolea, hukata tamaa akakufuru.⁹

3 Mnyenyekeeni Mwenyezi Mungu na huku mnamwomba akusameheni dhambi zenu. Kisha rejeeni kwake kwa kumuabudu kwa ikhlasi na vitendo vyema, ili apate kukustarehesheni starehe nzuri duniani mpaka utakapo kufikieni muda wenu uliyo kadiriwa, na apewe Akhera kila mwenye vitendo vyema malipo ya kazi yake na fadhila yake. Na pindi mkiyaacha haya ninayo kuitieni kwayo itakuwa mtajiletea adhabu. Na mimi nakukhofieni adhabu hii katika Siku Kubwa watakapo fufuliwa watu wote, na kutokea vitisho vikubwa kabisa!

4 Marejeo yenu ni kwa Mwenyezi Mungu peke yake hapa duniani na Siku ya Kiyama, atakapo kufufueni kutoka makaburini mwenu, ili akulipeni kwa vitendo vyenu. Na Yeye ni Muweza wa kila kitu. Kwani Yeye ndiye aliye kamilika uwezo wake, na hashindwi na kitu chochote.

5 Watu wanafunika vifua vyao kujaribu kuficha yanayo wapitia humo. Wanajitahidi kuficha, wakidai makusudio ya hayo ni kumficha Mwenyezi Mungu asijue hisiya za nyoyo zao! Hebu nawajue watu hawa kuwa hata wanapo kwenda kulala vitandani mwao, na wakavaa nguo zao za kulalia, na wakajisitiri na kiza cha usiku na usingizi, na kujifunika vifua, basi hapana shaka yoyote kuwa Mwenyezi Mungu anawajua, wakificha au wakitangaza. Kwani Yeye anayajua yaliyomo vifuani, na yanayo funikwa ndani yake.

6 Na wajue watu hawa kuwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na neema zake, na ujuzi wake, umeenea kila kitu. Basi hapana mnyama anaye furukuta katika ardhi ila Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake kesho mtengenezea riziki yake inayo wafikiana naye katika hali mbali mbali. Naye anajua anaka wapi katika hali ya uhai wake, na pahala atapo wekwa wakati wa kufa kwake! Kila kitu katika hayo kimekwisha dhibitiwa kwake *Subhanahu* katika Kitabu chenye kuweka wazi hali zote ziliomo.

7 Na Mwenyezi Mungu kaziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yake katika siku sita. Na kabla ya hapo palikuwa hapana chochote zaidi kuliko ulimwengu wa maji, na juu yake A'rshi, Kiti cha Enzi cha Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ameumba ulimwengu wote huu ili adhihirishe kwa kukujaribuni hali zenu, enyi watu, atokeze kati yenu anaye mkubali Mwenyezi Mungu kwa ut'ifu na vitendo vyema, na nani anaye yaacha hayo...Na juu ya uwezo huu wa kuumba, ukiwaambia kwa yakini: Nyinyi mtafufuliwa kutoka makaburini kwenu, na kwamba wao wameumbwa ili wafe na wafufuliwe, wao mbio mbio wanakurudi kwa mkazo kuwa haya mliyo kuja nayo hayana ukweli wowote! Wala hayo si chochote ila ni kama uchawi ulio wazi wa kuchezea akili tu.

8 Iliyoy kuwa hikima yetu ni kuakhirisha adhabu ya ukafiri wao hapa duniani mpaka wakati tuliyo uweka, nao ni Siku ya Kiyama, wao husema kwa kejeli: Nini kinacho mzuia hivi sasa? Na ailete hiyo adhabu ikiwa anasema kweli katika hiyo ahadi yake! Basi nawajue hao kwamba adhabu itakuja tu bila ya muhali. Na itapo wajia hawatapata kuokoka, na itawazunguka kwa sababu ya kejeli zao na kutaka kuvunja hishima.

9 Na katika tabia za binaadamu ni kujizamisha mwenyewe katika hali aliyo nayo. Basi tukimpa baadhi ya neema na rehema, kama vile afya nzuri, na ukunjufu wa riziki, kisha baadae tukamwondolea neema hizo,

10. Na tukimwonjesha neema baada ya madhara yaliyo mpata husema: Taabu zimekwisha niondokea. Hakika yeye hujitapa na kutafakhari.¹⁰

11. Ila wale walio subiri wakatenda mema. Hao watapata msamaha na ujira mkubwa.¹¹

12. Basi labda utaacha baadhi ya yale yaliyo funuliwa kwako, na kifua kitaona dhiki kwa hayo, kwa sababu wanasema: Mbona hakuteremshiwa khazina, au wakaja naye Malaika? Wewe ni mwenyaji tu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa kila kitu.¹²

13. Au wanasema: Ameizua? Sema: Basi leteni Sura kumi zilizo zuliwa mfano wa hii, na waiteni muwawezao badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli.¹³

14. Na wasipo kuitikieni, basi jueni ya kwamba (hii Qur'ani) imeteremshwa kwa ujuzi wa Mwenyezi Mungu, na kwamba hapana mungu ila Yeye. Basi je! Nyinyi ni Waislamu?¹⁴

15. Wanao taka maisha ya dunia na pumbao lake tutawalipa humo vitendo vyao kaamili. Na wao humo hawatopunjwa.¹⁵

16. Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu Akhera ila Moto, na yataharibika waliyo yafanya, na yatapotea bure waliyo kuwa wakiyatenda.¹⁶

17. Basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola wake Mlezi, inayo fuatwa na shahidi anaye toka kwake, na kabla yake kilikuwa Kitabu cha Musa kilicho kuwa mwongozi na rehema - hao wanamuamini, na anaye mkataa katika makundi, basi

kwa mujibu wa mipango yetu, yeye hupita mipaka katika kukata tamaa kuwa neema hiyo haitorudi tena; na akapita mipaka katika kuzikufuru neema nyengine ambazo bado angali anastarehe nazo.

10 Na tukimpa neema baada ya shida aliyo kuwa nayo yeye husema: Shida zangu zote zimekwisha niondokea, wala hazitarudi tena! Na hayo humpelekea upeo wa kufurahikia starehe za dunia, na kujifakhrisha bila ya kiasi. Moyo wake huwa umeshughulika, usimshukuru Mola wake Mlezi! Hii ndiyo hali ya binaadamu wengi, wanababaika baina ya kukata tamaa na kujitapa!

11 Na aibu hii hawaachi kuwa nayo ila wale wanao subiri wakati wa dhiki, na wakatenda mema wakati wa faraji na shida. Hawa watasamehewa dhambi zao, na watapata ujira mkubwa kwa vitendo vyao vyema.

12 Ewe Nabii! Usijaribu kutaka kuwaridhi washirikina, kwani hao hawaamini. Na huenda ukijaribu kutaka kuwaridhi ukaacha kusoma baadhi ya uliyo letewa Wahyi, katika yale wasiyo penda wao kuyasikia, kama vile kudharauliwa baadhi ya miungu yao, kwa kukhofu kuwa wasije wakakejeli! Na huenda pengine ukahisi dhiki unapo wasomea, kwa kuwa wao wanataka Mwenyezi Mungu akuteremshie khazina ustarehe nayo kama wafalme, au waje nawe malaika watwambie ukweli wake! Basi, ewe Nabii! Usizibali inadi zao. Kwani wewe si chochote ila ni mwenyaji na mhadharishaji wa adhabu za Mwenyezi Mungu kwa anaye kwenda kinyume na amri yake. Nawe hayo umefanya, basi jipumzisha nafsi yako nao. Na jua kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuangalia na kulinda kila kitu. Naye atawafanyia kama wanavyo stahiki.

13 Katika Qur'ani ipo Ishara inayo thibitisha ukweli wako. Basi wao wakisema, kuwa hii umeitunga wewe na umemzulia Mwenyezi Mungu, wewe waambie: Ikiwa Qur'ani hii imetokana na mwanaadamu, basi yamkinika mwanaadamu mwengine kuleta mfano wake. Na nyinyi ni mafasihi kuliko wote. Basi leteni Sura kumi kama hii mbali mbali, na mtakeni msaada yeyote mnaye weza kumtaka, katika watu na majini, kama hakika mnasema kweli katika hayo madai yenu kuwa haya ni maneno ya binaadamu. (Tazama Maelezo 11:13)

14 Mkishindwa, na wakashindwa mlio wataka msaada, kuleta mfano wake hii wa kuzua, basi jueni kuwa Qur'ani haikuteremshwa ila kwa kuambatana na ujuzi wake Mwenyezi Mungu. Ilimu yake haijui mtu ila Yeye. Na jueni kuwa hapana mungu ila Allah, Mwenyezi Mungu tu. Hapana anaye tenda kazi yake. Basi kuweni Waislamu baada ya kwisha thibiti hoja hizi juu yenu, kama nyinyi mnataka Haki.

15 Wenye kutaka uhai wa duniani, na kustarehea ladha zake na pumbao lake, tutawapa matunda ya vitendo vyao bila ya nuksani.

16 Hao ambao hima yao ni kushughulikia dunia tu, Akhera hawana lao jambo ila adhabu ya Motoni, na kuharibikiwa na yote waliyo yafanya duniani, kwa sababu hawakuwa na fungu lolote katika Akhera. Na hayo wayatendayo pia yatakuwa yameharibika vile vile, kwani kitendo kisicho leta mafanikio ya daima ni kama kwamba hakikupata kuwoko.

Moto ndio pahala pa miadi yao. Basi usiwe na shaka juu ya hayo. Hii ni Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi; lakini watu wengi hawaamini.¹⁷

18. Na nani aliye dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye mzulia Mwenyezi Mungu uwongo? Hao watahudhurishwa mbele ya Mola wao Mlezi, na mashahidi watasema: Hawa ndio walio mtungia uwongo Mola wao Mlezi. Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate walio dhulumu,¹⁸

19. Ambao wanazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu, na wanaitakia ipotoke, na wanaikataa Akhera.¹⁹

20. Hao hawawezi kushinda katika ardhi, wala hawana walinzi isipo kuwa Mwenyezi Mungu. Watazidishiwa adhabu. Hawakuwa wakiweza kusikia wala hawakuwa wakiona.²⁰

21. Hao ndio walio zikhasiri nafsi zao, na yakawapotea waliyo kuwa wakiyazua.²¹

22. Bila ya shaka hakika wao ndio wenye kukhasiri huko Akhera.²²

23. Hakika wale walio amini, na wakatenda mema, na wakanyenyekea kwa Mola wao Mlezi, hao ndio watu wa Peponi, na humo watadumu.²³

24. Mfano wa makundi mawili ni kama kipofu kiziwi, na mwenye kuona na anasikia.

17 Je, anaye kuwa anakwenda katika maisha yake kwa uangalifu na uwongofu kutokana na Mola wake Mlezi, na anaitaka Haki kwa kuifanyia ikhlasi, pamoja naye anaye shahidi anaye mshuhudia kuwa kweli katoka kwa Mwenyezi Mungu, naye shahidi huyo ni Qur'ani, na shahidi wa kabla yake ni Kitabu cha Musa alichokiteremsha Mwenyezi Mungu kiwe ni uwongozi wa kufuatwa kwa aliyo yaleta, na ni rehema kwa wenye kukifuata, je, huyo ni sawa sawa na anaye kwenda katika maisha yake katika giza na upofu, hashughulikii ile starehe za duniani tu na pumbao lake? Hao walio tajwa mwanzo ndio wale ambao Mwenyezi Mungu ameyatia nuru macho yao. Wanamuamini Nabii huyu, na Kitabu alichokiteremshiwa. Na wenye kumkataa wakakusanyika na kujiunga dhidi yake, basi Moto ndio pahali pa miadi yao Siku ya Kiyama. Ewe Nabii! Usiwe na shaka na hii Qur'ani. Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Haingii upotovu. Lakini watu wengi wanapotezwa na matamano, basi hawaamini kama iwapasavyo. (*Tazama Maelezo 11:17*)

18 Hapana walio zidi kujidhulumu nafsi zao na wakajitenga mbali na Haki kuliko wale wanao tunga uwongo, na kisha wakamnasibishia Mwenyezi Mungu. Hakika watu hawa Siku ya Kiyama wataadhibiwa mbele ya Mola wao Mlezi awahisabie kwa yale maovu waliyo yatenda. Mashahidi miongoni mwa Malaika, na Manabii, na wengineo, watasema: Hawa ndio walio tenda makosa maovu kabisa na dhulma kwa mintarafu ya Muumba wao! Hapana shaka laana ya Mwenyezi Mungu itawapata hao kwa kuwa ni wenye kudhulumu.

19 Hawa ndio wanawagezu watu wasiifuate Dini ya Mwenyezi Mungu, na wanawazuia. Nayo hiyo ndiyo Njia yake Iliyo Nyooka. Na wanataka Njia hii iwafikiane na matamano yao na pumbao lao, kwa hivyo yende upogo. Hao wanaikanya Akhera, na yaliyomo ndani ya kulipwa thawabu Muumini na kuadhibiwa kafiri.

20 Hao makafiri hawana nguvu za kumshinda Mwenyezi Mungu asiwatie nguvuni duniani akawaadhibu; na hawana wasaidizi wa kuweza kuwakinga na adhabu yake pindi Mwenyezi Mungu akitaka kuwaletea hiyo katika Akhera, hata ikiwa mardufu ya ile ambayo wangelipata duniani, ingeli kuwa Mwenyezi Mungu anataka iwafikie. Kwa sababu hao wamechukia kuisikia Qur'ani, na kuzingatia Ishara za Mwenyezi Mungu katika ulimwengu. Wamekuwa kama kwamba hawakuwa wakiweza kusikia wala kuona.

21 Hao makafiri hawapati faida yoyote katika kumuabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu! Bali wamejikhasiri nafsi zao, na huko Akhera huo uwongo walio kuwa wakiuzua, na madai ya upotovu, na miungu ya uwongo waliyo kuwa wakiiunda, na wakadai kuwa hiyo ati ikiwafaa au itawaombea - yote hayo yatawapotea. Kwa sababu hakika Siku ya Kiyama ndiyo Siku ya hakika, ambayo haina udanganyifu wala uzushi.

22 Kweli, hakika wao Siku ya Akhera ndio wenye kukhasiri kuliko watu wote!

23 Bila ya shaka wale wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wakatenda a'mali njema, na nyoyo zao zikanyenyekea na zikatua kuikubali hukumu ya Mola wao Mlezi, hao ndio wanao stahiki kuingia Peponi na kudumu humo milele.

Je, wawili hawa wanakuwa sawa kwa kufananishwa? Basi, je, hamfikiri?²⁴

25. Na Sisi tulimtuma Nuhu kwa watu wake, akawaambia: Hakika mimi ni mwonyaji kwenu ninaye bainisha,²⁵

26. Ya kwamba msimuabudu isipo kuwa Mwenyezi Mungu tu. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku Chungu.²⁶

27. Na wakasema wakuu walio kufuru katika kaumu yake: Hatukuoni wewe ila ni mtu tu kama sisi, wala hatukuoni wamekufuata ila wale walio kuwa kwetu watu duni, wasio kuwa na akili. Wala hatukuoneni kuwa mna ubora wowote kutushinda sisi. Bali tuna hakika nyinyi ni waongo.²⁷

28. Akasema: Enyi watu wangu! Hebu fikirini! Ikiwa mimi ninayo hoja wazi iliyo toka kwa Mola wangu Mlezi, na amenipa rehema kutoka kwake, nayo ikakufichikieni; je, tukulazimisheni kuikubali hali nyinyi mnaichukia?²⁸

29. Na enyi watu wangu! Mimi sikuombeni mali kwa ajili ya haya. Mimi sina ujira ila kwa Mwenyezi Mungu; na mimi sitawafukuza walio amini. Hakika wao watakutana na Mola wao Mlezi, lakini mimi nakuoneni mnaifanya ujinga.²⁹

30. Na enyi watu wangu! Ni nani atakaye nisaidia kwa Mwenyezi Mungu nikiwafukuza hawa? Basi je, hamfikiri?³⁰

31. Wala sikwambiini kuwa nina khazina za Mwenyezi Mungu; wala kuwa mimi najua mambo ya ghaibu; wala sisemi: Mimi ni Malaika. Wala siwasemi wale ambao

24 Mfano wa makundi mawili hayo, ya Waumini na makafiri, ni kama kipofu anaye kwenda bila ya uwongofu na kiziwi asiye sikia uwongozi wa kuokoka, na kundi la pili ni kama mwenye macho anaye iona njia ya kheri na uokofu, na mwenye masikio makali anaye sikia kila lenye manufaa naye. Makundi mawili hayo hayawezi kuwa sawa katika hali yao na kuishia kwao! Basi, enyi watu, hamfikiri yaliyo baina yenu ya khitilafu ya utambuzi na ukafiri, na khitilafu baina ya baat'ili na Haki, mkawa mbali na njia ya upotovu, na mkaishika Njia Iliyo Nyooka?

25 Na kama tulivyo kutuma kwa watu wako uwaonye na uwabashirie kheri, wakakubali baadhi yao kwa inadi na upinzani, kadhaalika tulimtuma Nuhu kwa watu wake, akawaambia: Mimi nakuhadharisheni na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na nakuonyesheni njia ya kuokoka.

26 Akawaambia: Mimi nilitakalo kwenu ni kuwa msimuabudu ila Mwenyezi Mungu tu, kwa sababu nakukhofieni, mkimuabudu mwenginewe au mkimshirikisha pamoja naye wenginewe katika kumuabudu, isije ikakufikieni siku ya adhabu yake yenye machungu makali.

27 Wakuu wa kaumu yake wakasema: Sisi hatukuoni wewe ila kuwa ni mtu kama sisi. Hapana lolote linalo kufanya uwe namna ya peke yako, au uwe na ubora wa kutupelekea tukuamini kuwa wewe ni Mtume utokaye kwa Mwenyezi Mungu! Na wala hatuwaoni hao walio kufuata ila ni watu wa t'abaka la chini miongoni mwetu! Wala hatukuoneni nyinyi kuwa ni bora kuliko sisi! Bali sisi tunaitakidi kuwa nyinyi ni waongo tu katika hayo mnayo dai.

28 Nuhu akasema: Enyi watu! Hebu nambieni, ikiwa mimi naungwa mkono na hoja zilizo wazi kutokana na Mola wangu Mlezi, naye akanipa kwa rehema yake Unabii na Utume, na nuru yake ikafichikana kwenu, na kughurika kwenu kwa cheo na mali kukakutieni upofu msizone, basi je, itafaa tukulazimisheni mziamini hoja kwa nguvu na karaha?

29 Enyi watu! Mimi sitaki mali kwa kufikisha Ujumbe wa Mola wangu Mlezi, bali nataraji malipo yangu kwa Mwenyezi Mungu. Wala mimi siwafukuzi kwenye baraza yangu na kuingiana nami walio muamini Mola wao Mlezi, kwa sababu ya kuwa nyinyi mnawadharau tu! Kwani wao watakuja kukutana na Mola wao Mlezi Siku ya Kiyama na watanishitaki kwake ikiwa nimewafukuza kwa ajili ya ufakiri wao. Lakini mimi nakuoneni nyinyi ni watu msio jua nini kinacho watukuza viumbe mbele ya Mwenyezi Mungu! Ni utajiri na cheo kama mnavyo dai, au kufuata Haki na kufanya kheri?

30 Enyi watu! Hapana yeyote awezaye kunikinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu nikiwafukuza hao hali nao ni wenye kumuamini Yeye. Je, bado mngali mnashikilia ujinga wenu? Hamkumbuki basi kuwa hawa watu wanaye Mola wao Mlezi wa kuwalipia?

yanawadharau macho yenu kuwa Mwenyezi Mungu hatawapa kheri - Mwenyezi Mungu anajua yaliomo katika nafsi zao - hapo bila ya shaka ninge kuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.³¹

32. Wakasema: Ewe Nuhu! Umejadiliana, na umekithirisha kutujadili. Basi tulettee hayo unayo tuahidi, ukiwa miongoni mwa wasemao kweli.³²

33. Akasema: Mwenyezi Mungu atakuleteeni akipenda. Wala nyinyi si wenye kumshinda.³³

34. Wala nasaha yangu haikufaini kitu nikitaka kukunasihini, ikiwa Mwenyezi Mungu anataka kukuachieni mpotee. Yeye ndiye Mola wenu Mlezi; na kwake mtarejeshwa.³⁴

35. Au ndio wanasema: Ameizua? Sema: Ikiwa nimeizua, basi kosa hilo ni juu yangu, na mimi sikhusiki na makosa myatendayo.³⁵

36. Na akafunuliwa Nuhu akaambiwa: Hataamini yeyote katika watu wako ila wale walio kwisha amini. Basi usisikitike kwa waliyo kuwa wakiyatenda.³⁶

37. Na unda jahazi mbele ya macho yetu na kwa mujibu wa ufunuo wetu. Wala usinisemeze kuwatetea walio dhulumu. Kwani hao bila ya shaka watazamishwa.³⁷

38. Na akawa anaunda jahazi, na kila wakipita wakuu wa kaumu yake wakimkejeli. Yeye akasema: Ikiwa nyinyi mnatukejeli na sisi tunakukejelini kama mnavyo tukejeli.³⁸

31 Wala sikwambiini kuwa kwa sababu mimi ni Mtume, basi ninazo khazina za riziki ya Mwenyezi Mungu, nitumie nitakavyo, na kwa hivyo nimfanye anaye nifuata tajiri! Wala sikwambiini kuwa mimi najua mambo ya ghaibu, na kwa hivyo nikupeni khabari yale yaliyo mkhusu Mwenyezi Mungu tu kuyajua, kwa kuwa hapana mja yeyote anaye yajua! Wala mimi sikwambiini kuwa mimi ni Malaika, na kwa hivyo mnirudi kwa kauli yenu: Huyu si chochote ila mwanaadamu tu! Wala siwasemi wale mnao wadharau kwamba Mwenyezi Mungu hatowapa kheri yoyote kwa kutaka kuridhi myatakayo! Kwani Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anaye jua ikhlasi iliomo katika nafsi zao!..Mimi nikisema myatakayo nitakuwa katika wenye kujidhulumu na kudhulumu wengineo.

32 Wakasema: Ewe Nuhu! Umebishana nasi ili tukuamini, na umezidisha kutujadili mpaka tumechoka. Sasa hatuyastahamili tena maneno yako. Basi, hebu, tulettee hiyo adhabu unayo tutishia, kama wewe kweli unayo yasema kwamba Mwenyezi Mungu atatuadhibu tukito kuamini!

33 Nuhu akasema: Mambo haya yamo mikononi mwa Mwenyezi Mungu pekee. Yeye ndiye atakuleteeni alitakalo kwa hikima yake. Wala nyinyi hamwezi kuikimbia adhabu yake itakapo kuja. Kwani Yeye, *Subhanahu*, haemewi na chochote katika ardhi wala katika mbingu.

34 Wala nasaha yangu haitakufaeni kitu kwa kuwa tu nakutakieni kheri, ikiwa Mwenyezi Mungu anakutakeni mpotee kwa mujibu wa ilimu yake na uwezo wake kwa kuharibika nyoyo zenu, hata zimekuwa haziikubali Haki! Yeye *Subhanahu* ndiye Mola wenu Mlezi, naye atakurejesheni kwake Siku ya Kiyama. Na atakulipeni kwa mlivyo kuwa mkitenda.

35 Nini msimamo wa washirikina kukhusu hadithi hizi za kweli? Watasema kazizua? Wakisema hivyo, basi waambie: Ikiwa nimezizua kama mnavyo dai, basi hilo ni kosa kubwa; ni juu yangu mimi tu dhambi zake! Na ikiwa nimesema kweli, basi nyinyi ndio wenye makosa, na mimi sikhusiki na matokeo ya makosa yenu.

36 Mwenyezi Mungu akamletea wahyi Nuhu akamwambia: Hatakusadiki wala hataifuata Haki yeyote katika kaumu yako baada ya sasa, isipo kuwa wale walio kwisha tangulia kukuamini kabla ya hayo. Basi ewe Nuhu! Usihuzunike kwa sababu ya waliyo kuwa wakikutendea, ya kukukadhibisha, na kukuudhi. Kwani Sisi tutawalipiza karibu.

37 Tukamwambia: Tengeneza chombo chini ya uangalizi na ulinzi wetu, wala usinisemeze kwa ajili ya hawa madhaalimu, kwa sababu nilikwisha itikia ombi lako, na nimekwisha amrisha wateketezwe kwa kuzamishwa. (*Tazama* aya ya 27, Sura ya 23 Al-Muuminun)

38 Nuhu akaingia kujenga chombo. Kila wakipita waongozi wa makafiri katika kaumu yake wakimfanyia maskhara, kwa ujinga wao na kuwa hawajui nini anacho kusudia! Nuhu akawaambia: Mkitufanyia maskhara sisi kwa kutojua kwenu ukweli wa ahadi ya Mwenyezi Mungu, basi hakika sisi pia tutakufanyieni maskhara, kama mnavyo tufanyia sisi.

- 39.** Nanyi mtakuja jua ni nani itakaye mfikia adhabu ya kumhizi, na itakaye mteremkia adhabu ya kudumu.³⁹
- 40.** Hata ilipo kuja amri yetu, na tanuri ikafoka maji, tulisema: Pakia humo wawili wawili, dume na jike, kutoka kila aina, na ahali zako, isipo kuwa wale ambao imekwisha wapitia hukumu; na watu walio amini. Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.⁴⁰
- 41.** Na akasema: Pandeni humo kwa Bismillahi, Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, kwenda kwake na kusimama kwake. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.⁴¹
- 42.** Ikawa inakwenda nao katika mawimbi kama milima. Na Nuhu akamwita mwanawe naye alikuwa mbali: Ewe mwanangu! Panda pamoja nasi, wala usiwe pamoja na makafiri.⁴²
- 43.** Akasema: Nitakimbilia mlimani unilinde na maji. (Nuhu) akasema: Leo hapana wa kulindwa na amri ya Mwenyezi Mungu ila aliye mrehemu mwenyewe. Na wimbi likawatenganisha, akawa katika walio zama.⁴³
- 44.** Na ikasemwa: Ewe ardhi! Meza maji yako. Na Ewe mbingu! Jizuie. Basi maji yakadidimia chini, na amri ikapitishwa, na (jahazi) likasimama juu ya (mlima) wa Al Juudiy. Na ikasemwa: Wapotelee mbali watu walio dhulumu!⁴⁴
- 45.** Na Nuhu alimwomba Mola wake Mlezi: Ee Mola Mlezi wangu! Hakika mwanangu ni katika ahali zangu, na hakika ahadi yako ni haki. Na Wewe ni Mwenye haki kuliko mahakimu wote.⁴⁵

39 Mtakuja jua nani kati yetu atakaye fikiwa na adhabu ya kumdhalilisha, na atafikiwa na adhabu ya kudumu milele katika Akhera!

40 Hata ulipo wadia wakati wa amri yetu ya kuwahilikisha, yalikuja maji kwa nguvu yakifoka na kutoa mapovu, kama maji yanavyo tokota juu ya moto. Tukamwambia Nuhu: Wapakie nawe katika hiyo Safina kutoka kila namna ya wanyama dume na jike. Na pia wapakie humo ahali zako, yaani watu wa nyumbani kwako, isipokuwa ilio kwisha pita juu yake hukumu yetu ya kumteketeza. Na pia kadhaalika wapakie humo katika watu wako walio amini. Na hao hawakuwa ila idadi chache tu.

41 Na baada ya kwisha liweka tayari jahazi Nuhu aliwaambia watu wake: Pandeni humo kwa kujipigia feli njema kwa kulitaja jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu (kupiga *BISMILLAHI*) wakati wa kwenda na wakati wa kusimama, na wakati wa kuingia na wakati wa kutoka humo. Na muombeni Mwenyezi Mungu akusameheni kwa madhambi mlio tenda, na akurehemuni. Kwani maghfira na rehema ni katika shani yake *Subhanahu wa Taa'la*.

42 Wakaingia katika Safina, ikawa inakwenda katika mawimbi makubwa makubwa kama milima! Na ilipo anza kwenda Nuhu alimkumbuka mwanawe kwa huruma ya baba, naye alikuwa yuko mbali kajitenga na wito wa baba yake. Akamwita: Ewe mwanangu! Panda nasi, wala usiwe katika wanao ikataa Dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu!

43 Mtoto hakumt'i baba yake mwenye kumwonea huruma! Akasema: Nitakwenda pahala pa kunilinda na maji! Baba, mwenye kujua hukumu ya Mwenyezi Mungu kwa wenye kuasi, alisema: Ewe mwanangu! Hakipatikani cha kuzuia hukumu ya Mwenyezi Mungu ya kuwazamisha walio dhulumu! Basi yule kijana akapotea kwenye macho ya baba yake anaye mnasih nyuma ya wimbi lililo panda juu; akawa pamoja na wakanushao, walio zama, walio teketea.

44 Walipo kwisha hiliki makafiri kwa kuzamishwa, ikaja amri ya Mwenyezi Mungu ya maumbile. Ikasemwa kwa hukumu ya uumbaji: Ewe ardhi! Yameze maji yako, na wewe mbingu! Sita na kuteremsha maji. Yakaondoka maji kwenye ardhi, wala kisiongezeke chochote kutoka mbinguni. Hukumu ya Mwenyezi Mungu ya kuhiliki ikamalizika. Jahazi likatua na likasimama juu ya mlima uitwao Al Juudiy. Na Mwenyezi Mungu akawahukumia walio dhulumu kwa kuwatenga na rehema yake. Ikasemwa: Wateketee kaumu walio dhulumu kwa sababu ya dhulma zao. (*Tazama Maelezo 11:44*)

45 Huruma ilimshika Nuhu moyoni mwake kwa ajili ya mwanawe. Akamwomba Mola Mlezi wake kwa

46. Akasema: Ewe Nuhu! Huyu si katika ahali zako. Mwendo wake si mwema. Basi usiniombe jambo usio na ujuzi nalo. Mimi nakuwaidhi usije ukawa miongoni mwa wajinga.⁴⁶

47. Nuhu akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Mimi najikinga kwako nisikuombe nisio na ujuzi nalo. Na kama hunisamehe na ukanirehemu, nitakuwa katika walio khasiri.⁴⁷

48. Ikasemwa: Ewe Nuhu! Shuka kwa salama itokayo kwetu, na baraka nyingi juu yako na juu ya watu walio pamoja nawe. Na zitakuwapo kaumu tutakazo zistarehesha, na kisha zitashikwa na adhabu chungu itokayo kwetu.⁴⁸

49. Hizi ni katika khabari za ghaibu tunazo kufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii. Basi subiri! Hakika Mwisho ni wa wachamngu.⁴⁹

50. Na kwa kina A'adi tulimtuma ndugu yao Hud. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu! Nyinyi hamna mungu isipo kuwa Yeye. Nyinyi si chochote ila ni wazushi tu.⁵⁰

51. Enyi watu wangu! Sikuombeni ujira kwa ajili ya haya. Haukuwa ujira wangu ila kwa Yule aliye niumba. Basi hamtumii akili?⁵¹

52. Na enyi watu wangu! Muombeni msamaha Mola wenu Mlezi, kisha mtubie kwake.

unyeyekevu na kuona huruma, akasema: Ewe Muumba wangu, uliye nianzisha nami sijawa chochote! Hakika huyu mwanangu ni kipande cha nafsi yangu, naye ni katika ahali zangu. Na Wewe umeahidi kuwa utawaokoa ahali zangu, na ahadi yako ni ya kweli, madhubuti, lazima iwe. Na hapana muadilifu kama Wewe! Kwani Wewe ndiye Mjuzi kushinda wote, na Wewe ni mwingi wa hikima kuliko wote wenye kuhukumu!

46 *Allah Subhanahu* akasema: Hakika huyo mwanao si katika ahali zako. Kwani yeye kwa ukafiri wake na mwendo wake pamoja na makafiri amekata makhusiano baina yako na yeye. Naye ametenda vitendo visio vyema. Kwa hivyo amekuwa si katika wewe. Nawe usitake jambo usilo lijua, kuwa ndilo au silo. Wala usende kufuata huruma zako. Na mimi nakuongoza njia ya Haki ili usiwe katika wajinga ukasahau kwa huruma zako Hakika iliyo thibiti!

47 Nuhu akasema: Ewe Muumba wangu, uliye tawala mambo yangu yote! Mimi nakuangukia Wewe. Sitakuomba nisicho kijua hakika yake. Nawe nisamehe kwa niliyo yasema kutokana na huruma zangu. Kama hukunipa fadhila ya msamaha wako, na ukanirehemu kwa rehema yako, nitakuwa katika makundi ya walio khasiri.

48 Akaambiwa kwa wahyi: Ewe Nuhu! Teremka nchi kavu kutokana na hiyo Safina ya uwokovu, salama usalimina, kwa amani itokanayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na baraka nyingi zitokazo kwa Mwenyezi Mungu juu yako na juu ya hao walio pamoja nawe, ambao watakuja kuwa mataifa mbali mbali baada yako. Na baadhi yao watapata baraka ya Imani na ut'iifu, na baadhi yao watakuwa watu wanao itaka starehe ya dunia, na watapata starehe yake bila ya kuit'ii Haki. Kisha Siku ya Kiyama itawapata adhabu chungu na kali.

49 Hizo ni simulizi tulizo kusimulia wewe, ewe Nabii, juu ya Nuhu na kaumu yake. Hizo ni khabari za ghaibu ambazo hazijui ila Mwenyezi Mungu. Wewe wala watu wako hamkuwa mkizijua kwa namna hii, na kwa tafsili hii, kabla ya wahyi huu. Basi wewe vumilia maudhi ya watu wako, kama walivyo subiri Manabii wa kabla yako. Kwani mwisho wako ni kufuzu kama ulivyo kuwa mwisho wao hao. Na Mwisho mwema daima ni wa wale wanao iogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kuamini na kutenda vitendo vyema.

50 Na Sisi tuliwapelekea Kaumu ya A'adi wa mwanzo ndugu yao katika kabila yao, naye ni huyo Hud. Akawaambia: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu pekee. Kwani hamna anaye stahiki kuabudiwa isipo kuwa Yeye. Na nyinyi si cho chote ila mnazua uwongo tu kudai kuwa Mwenyezi Mungu ana washirika wanao stahiki nao kuabudiwa ili wawe waombezi wenu kwa Mwenyezi Mungu! (*Tazama* maelezo ya ki-ilimu juu ya aya 65, Sura ya 7 Al-A'araaf)

51 Enyi watu! Kwa nasaha hii sitaki kwenu kulipwa kwa cheo, au utawala, au mali. Kwani ujira wangu uko kwa Mwenyezi Mungu aliye niumba. Wala haikufaliini nyinyi mkawa mmechotwa akili zenu kwa kughafilika msitambue linalo kufaeni na linalo kudhuruni!

Atakuleteeni mbingu zenye kunyesha mvua ya kumiminika, na atakuzidishieni nguvu juu ya nguvu zenu. Wala msigeuke mkawa wakosefu.⁵²

53. Wakasema: Ewe Hud! Hujatuletea dalili wazi. Wala sisi hatuiachi miungu yetu kwa kufuata kauli yako. Na wala sisi hatukuamini wewe.⁵³

54. Sisi tunasema: Baadhi katika miungu yetu imekusibu kwa baa. Akasema: Hakika mimi namshuhudisha Mwenyezi Mungu, na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnao wafanya washirika,⁵⁴

55. Mkamwacha Yeye. Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi, na kisha msinipe muhula!⁵⁵

56. Hakika mimi nimentegemea Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye anamwendesha atakavyo. Hakika Mola wangu Mlezi yuko juu ya Njia Iliyo Nyooka.⁵⁶

57. Na ikiwa watarudi nyuma, basi mimi nimekwisha kufikishieni niliyo tumwa kwenu. Na Mola wangu Mlezi atawaleta watu wengine badala yenu, wala nyinyi hamumdhuru kitu Yeye. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye kuhifadhi kila kitu.⁵⁷

58. Ilipo fika amri yetu, tulimwokoia Hud na walio amini pamoja naye, kwa rehema itokayo kwetu. Na tukawaokoa na adhabu ngumu.⁵⁸

59. Na hao ndio kina A'adi. Walizikanusha Ishara za Mola wao Mlezi, na wakawaasi Mitume wake, na wakafuata amri ya kila jabari mwenye inda.⁵⁹

52 Enyi watu! Mtakeni aliye kuumbeni akusameheni madhambi yaliyo kwisha tangulia. Kisha rejeeni kwake. Hapana shaka mkifanya hayo atakuleteeni mvua nyingi mfululizo, basi zitaongezeka kheri zenu, na zitazidi nguvu zenu juu ya nguvu mnazo jivunia sasa! Wala msiyawache haya ninayo kuiteni muyafwate, mkashikilia maasi ambayo yatakuangamizeni kwenye hilaki.

53 Wakasema: Ewe Hud! Hukutuletea hoja yoyote iliyo wazi ya kuonyesha ukweli wa hayo unayo tuitia. Wala sisi hatutoacha kuabudu miungu yetu kwa kufuata kauli yako tu! Je, tuwawache hao, na hali sisi hatukusadiki wewe?

54 Na hatuna la kusema juu ya msimamo wako nasi ila kuwa mmojapo katika miungu yetu imekupatiliza kwa shari, ndio maana ukawa unaropokwa maneno haya! Naye akasema naye ameshikilia Imani yake na anawapinga: Ninasema, na namshuhudisha Mwenyezi Mungu kwa haya niyasemayo, na nakushuhudisheni nyinyi, ya kwamba mimi najitenga mbali kabisa na maradhi ya ushirikina mliyo nayo. Kwani nyinyi ni wagonjwa!

55 Wala mimi sikujalini, wala siwajali miungu yenu hiyo ambayo mnadai kuwa imenipatiliza kwa uovu! Basi saidianeni, nyinyi na miungu yenu, kunifanyia vitimbi. Kisha wala msiakhirishe hiyo adhabu yenu kwangu hata dakika moja, kama mnaweza!

56 Mimi namtegemea Mwenyezi Mungu. Na Yeye ndiye Mwenye mamlaka juu ya mambo yangu na mambo yenu. Wala hashindwi na kitu chochote katika kupinga vitimbi vyenu. Na Yeye ni Muweza wa kila kitu. Basi hapana kiumbe yoyote ila yuko chini ya madaraka yake, na Yeye ndiye Mwenye kumsarifu atakavyo. Basi Yeye hashindwi na kunilinda na maudhi yenu, wala hashindwi kukuangamizeni! Hapana shaka vitendo vya Mola wangu Mlezi vinafuata njia ya Haki na Uadilifu katika ufalme wake. Yeye huwanusuru Waumini watendao mema, na huwahizi makafiri waharibifu.

57 Na mkiukataa wito wangu, basi kukataa kwenu hakunidhuru kitu. Na mwisho mbaya utakuwa wenu. Kwani mimi nimekwisha kufikishieni ujumbe aliyote nituma Mwenyezi Mungu kwenu. Na sina jukumu ila kufikisha tu. Na Mwenyezi Mungu atakuangamizeni nyinyi, na awaleta watu wengine wachukue majumba yenu na mali yenu! Na nyinyi hamumdhuru kitu chochote Yeye kwa kukataa kwenu kumuabudu! Hakika Mola wangu Mlezi ni Mlinzi wa kila kitu, Mwenye kujua kila kitu. Basi hapana katika mtendalo linalo fichikana kwake, wala haghafiliki kukutieni nguvuni.

58 Na ilipo kuja amri yetu ya kuwahiliki qaumu ya A'adi tulimwokoia Hud, na walio amini pamoja naye, kutokana na adhabu ya upepo mkali ulio wahiliki, na tukawaokoa na adhabu kubwa ya duniani na Akhera. Na hayo ni kwa sababu ya rehema yetu juu yao, kwa kuwawezesha kushika Imani.

59 Hao, basi, ndio kina A'adi! Walizikataa hoja zote zilizo wazi, na wakawaasi Mitume wote wa

60. Na wakafuatishiwa laana katika dunia hii na Siku ya Kiyama. Basi tambueni mtanabahi! Hakika kina A'adi walimkufuru Mola wao Mlezi. Na tambueni mtanabahi kuwa hakika waliangamizwa kina A'adi, kaumu ya Hud.⁶⁰

61. Na kina Thamud tuliwapelekea ndugu yao Saleh. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo. Basi mwombeni msamaha, kisha mtubu kwake. Hakika Mola wangu Mlezi yupo karibu, anaitikia maombi.⁶¹

62. Wakasema: Ewe Saleh! Hakika kabla ya haya ulikuwa unatarajiwa kheri kwetu. Je, unatukataza tusiwaabudu waliyo kuwa wakiwaabudu baba zetu? Na hakika sisi tuna shaka na wasiwasi kwa hayo unayo tuitia.⁶²

63. Akasema: Enyi watu wangu! Mwaonaje ikiwa ninazo dalili zilizo wazi kutokana na Mola wangu Mlezi, naye akawa kanipa rehema kutoka kwake - je, ni nani atakaye ninusuru kwa Mwenyezi Mungu nikimuasi? Basi nyinyi hamtanizidishia ila khasara tu.⁶³

64. Enyi watu wangu! Huyu ngamia wa Mwenyezi Mungu ni Ishara kwenu. Basi mwacheni ale katika ardhi ya Mwenyezi Mungu; wala msinguse kwa ubaya, isije ikakuangamizeni adhabu iliyo karibu.⁶⁴

65. Wakamchinja. Basi (Saleh) akasema: Stareheni katika mji wenu muda wa siku

Mwenyezi Mungu, kwa vile kumuasi yule Mtume wao aliye tumwa kwao, na vile kumt'ii kila aliye kuwa jeuri na mwingi wa inda katika maraisi wao na wakubwa wao!

60 Kwa hivyo wakastahiki kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Malaika, na watu wote kupata laana ya hapa duniani, na laana ya kuwafuatia Siku ya Kiyama. Basi na atanabahi kila mwenye kujua khabari ya A'adi kwamba hao kina A'adi waliikataa neema ya Muumba wao kwao, wala hawakuishukuru kwa kumuamini Yeye peke yake. Kwa hivyo ndio wakawa wanastahili wafukuzwe kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu, na wateremshiwe maangamizo makali! Hebu zingatieni maangamizo yao kwa kumkadhibisha Hud!

61 Na kwa kina Thamud tulimtuma mmoja wao ambaye amefungana nao kwa nasaba na mapenzi, naye ni Saleh. Akawaambia: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu pekee. Nyinyi hamna anaye stahiki kuabudiwa isipo kuwa Yeye. Yeye ndiye aliye kuumbeni kwenye ardhi, na akakuwekeni muiimarishie, na muiteo mavuno ya kukufaeni kheri yake...Basi mwombeni Yeye apate kukusameheni makosa yenu yaliyo kwisha tangulia. Kisha mrejee kwake na majuto kwa mlivyo muasi, na mkubali kumtii, kila mnapo tumbukia katika madhambi. Hakika Mola wangu Mlezi yupo karibu kwa rehema, na Mwenye kupokea maombi kwa mwenye kutaka msamaha na kumwomba. (*Tazama maelezo ya ki-ilimu ya aya 73, Sura 7 Al A'raaf*).

62 Wakasema: Ewe Saleh! Hakika wewe ulikuwa kwetu mtu wa kutarajiwa mema, na kupendwa, na kutukuzwa katika nyoyo zetu, kabla ya haya unayo tuitia! Hivyo unatutaka tuache ibada waliyo kuwa wakiabudu baba zetu na tuliyo izoea sisi na wao? Hakika sisi tuna shaka na huo wito wako wa kumuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja. Haya ni mambo ya kukutilia shaka na dhana mbovu wewe na huo wito wako!

63 Akasema: Enyi watu wangu! Hebu nambieni: ikiwa mimi kwa haya ninayo kukuitieni kwayo nina ujuzi nayo vilivyo, na nina hoja za kunitia nguvu kutoka kwa Mola wangu Mlezi, na ikawa Mola wangu Mlezi kanipa mimi na nyinyi rehema itokayo kwake, nayo ni Unabii na Utume, vipi basi nende kinyume na amri yake, na nimuasi kwa kutofikisha ujumbe wake kwa sababu ya kukusikilizeni nyinyi? Na nani wa kuninusuru na kunisaidia kuikinga adhabu yake nikimuasi Yeye? Nyinyi hamwezi kuninusuru na kunikinga na adhabu yake. Basi hamtonizidishia ila kupotea na kuingia khasarani ni kikut'iini nyinyi, na nikamuasi Mola wangu na Mola wenu Mlezi.

64 Na enyi watu wangu! Huyu ngamia wa Mwenyezi Mungu; amemfanya awe ni alama kwenu ya kushuhudia ukweli wa haya ninayo kuleteeni. Kwani huyu ni namna mbali na hao mlio wazoea. Basi mwachieni ale katika ardhi ya Mwenyezi, kwani yeye ni ngamia wake, na ardhi ni yake. Wala msifikishie uovu wowote wa kumdhuru. Kwani mkifanya hivyo Mwenyezi Mungu atakuangamizeni kwa adhabu iliyo karibu.

tatu. Hiyo ni ahadi isiyo kuwa ya uwongo.⁶⁵

66. Basi ilipo kuja amri yetu tulimwokoia Saleh na wale walio amini pamoja naye kwa rehema yetu kutokana na hizaya ya siku ile. Hakika Mola wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu Mwenye kushinda.⁶⁶

67. Na ukelele uliwaangamiza wale walio dhulumu, wakapambazukiwa nao ni maiti majumbani mwao.⁶⁷

68. Kama kwamba hawakuwako huko. Hebu zingatieni! Hakika kina Thamud walimkufuru Mola wao Mlezi. Hebu zingatieni! Thamud wamepotelea mbali!⁶⁸

69. Na wajumbe wetu walimjia Ibrahim kwa bishara njema, wakasema: Salama! Naye akasema: Salama! Hakukaa ila mara akaleta ndama wa kuchoma.⁶⁹

70. Basi alipoona mikono yao haimfikilii aliwatilia shaka, na akawaogopa. Wakasema: Usiogope! Hakika sisi tumetumwa kwa kaumu ya Lut'.⁷⁰

71. Na mkewe alikuwa kasimama wima, akacheka. Basi tukambashiria (kuzaliwa) Is-haq, na baada ya Is-haq Yaaqub.⁷¹

72. Akasema: Je, hivyo mimi nizae, na hali yangu ni kikongwe na huyu mume wangu ni kizee? Hakika haya ni mambo ya ajabu!⁷²

73. Wakasema: Je, unastaajabia amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na baraka zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye ndiye Msifiwa wa kutukuzwa.⁷³

65 Na wao wasiisikie nasaha yake, wala wasimkubalie. Kiburi chao na dharau yao iliwapelekea kumuwa yule ngamia. Basi yeye akawaambia: Stareheni na maisha yenu ya kilimwengu katika miji yenu muda wa siku tatu. Kisha baadae itakujieni adhabu ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ni ahadi ya kweli wala haina kinyume, wala haina uwongo ndani yake.

66 Ilipo kuja adhabu yetu tulimwokoia Saleh na wale walio amini pamoja naye kutokana na maangamizo kwa rehema iliyo toka kwetu khasa. Na tukawaokoa na hizaya na fedheha ya siku ya maangamizo ya Thamud. Hakika Mola wako Mlezi, ewe Nabii, ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda. Basi tuwa ukitegemea nguvu zake, na ushindi wake, na msaada wake, na nusra yake.

67 Ukelele uliwaangamiza kina Thamud kwa nguvu zake, na tetemeko lake, na ngurumo lake, kwa kuwa hao walijidhulumu wenyewe kwa ukafiri wao na uadui. Kulipo pambazuka wakawa katika majumba yao kimya, wamejinyoosha kifudufudi, maiti, hawatweti!

68 Mambo yao yakawaishia, na alama zao zikaondoka katika majumba yao. Wakawa kama kwamba hawajapata kuwamo humo. Hali yao ni ya kumzungua kila mwenye akili azingatie, na ajue kuwa hao kaumu ya Thamud walizikanya Ishara za aliye waumba!! Na kwa sababu ya hayo ndio wakaangamizwa na wakatengwa mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu.

69 Na Sisi tuliwatuma Malaika kwa Ibrahim wampe bishara njema yeye na mkewe kuwa watapata mwana. Waliwasalimu kwa kauli ya: Salama! Naye akarejesha amkio lao kwa kusema: Salama! Upesi upesi akenda kuwatengezea ndama aliye nona wa kuchoma ili wale.

70 Alipoona kuwa hawanyooshi mikono yao kama ada ya wageni akawatilia shaka kuwa hawa si wageni wa kawaida, na akahisi kuwa hawa ni Malaika. Ikamjia khofu kuwa isije kuwa kuja kwao ni kwa jambo ambalo halikumpendeza Mwenyezi Mungu, au kuwaadhibu watu wake. Wakasema, nao walijua athari ya ile khofu katika nafsi yake: Usiogope! Hakika sisi tumetumwa kuwahiliki kaumu Lut'.

71 Na mkewe alikuwa kasimama karibu akisikia maneno yao. Akacheka kwa furaha ya kuwa mwenyewe Lut', ambaye ni mtoto wa ndugu wa mumewe, atasalimika. Basi Sisi tulimbashiria kwa ndimi za wale Malaika kuwa atamzalia mumewe Ibrahimu mtoto mwanamume ataye itwa Is-haq, na huyo mtoto ataishi, na baadae Is-haq atampata Yaaqub.

72 Mke wa Ibrahim alipiga ukelele kwa kustaajabu: Ajabu gani hii, jamani! Nizae mimi kikongwe, na huyu mume wangu mnamuona kesho kuwa kizee kabisa! Kama huyu hapati mwana tena. Hakika haya ninayo yasikia ni mambo ya ajabu. Vipi vikongwe viwili kama mimi na mume wangu wazae tena?

73 Malaika wakamwambia: Unastaajabu nyinyi wawili kupata mwana kwa ajili ya uzee wenu? Haya yanatokana na amri ya Mwenyezi Mungu asiye shindwa na chochote. Hiyo ndiyo rehema ya Mwenyezi

74. Basi khofu ilipo mwondoka Ibrahim, na ikawa ile bishara imemfikia, alianza kujadiliana nasi juu ya kaumu ya Lut'.⁷⁴

75. Hakika Ibrahim alikuwa mpole, ana huruma, na mwepesi wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu.⁷⁵

76. (Akaambiwa): Ewe Ibrahim! Wachilia mbali haya! Kwa hakika amri ya Mola wako Mlezi imekwisha kuja, na hakika hao itawafikia adhabu isiyo rudi nyuma.⁷⁶

77. Na wajumbe wetu walipo kuja kwa Lut' aliwahuzunukia na akawaonea dhiki. Akasema: Hii leo ni siku ngumu!⁷⁷

78. Wakamjia kaumu yake mbio mbio. Na kabla ya haya walikuwa wakitenda maovu. Yeye akasema: Enyi watu wangu! Hawa binti zangu, ndio wametakasika zaidi kwenu. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, wala msinihizi mbele ya wageni wangu. Hivyo, hamna hata mtu mmoja miongoni mwenu aliye ongoka?⁷⁸

79. Wakasema: Bila shaka umekwisha jua hatuna haki juu ya binti zako, na unayajua tunayo yataka.⁷⁹

80. Akasema: Laiti ningeli kuwa na nguvu kwenu, au nategemea kwenye nguzo yenye nguvu!⁸⁰

81. (Wajumbe) wakasema: Ewe Lut'! Sisi ni wajumbe wa Mola wako Mlezi. Hawa hawatakufikia. Na wewe ondoka pamoja na ahali zako usiku ungalipo. Wala yeyote miongoni mwenu asitazame nyuma, isipo kuwa mkeo, kwani yeye utamfika msiba utakao wafika hao. Hakika miadi yao ni asubuhi. Je, asubuhi si karibu?⁸¹

Mungu. Na neema zake ni nyingi juu yenu wa ukoo wa Nabii. Basi hapana la ajabu nyinyi kupewa wasio pewa wenginewe. Mwenye kutenda hayo hakika anastahiki kuhimidiwa, ni mwingi wa hisani na ukarimu na upaji.

74 Zilipo mtoka khofu Ibrahim, na akaisikia bishara ya kumfurahisha ya kupata mwana, ikamwingia huruma, akaanza kujadiliana na wale wajumbe katika shauri la kuangamizwa kaumu Lut'.

75 Hakika Ibrahim ni mpole mno, hapendelei mapatilizio ya kwa haraka, mwingi wa kuungulika na kuona uchungu kwa shida zinao wapata watu, tena yeye ni mwenye kutubu na kurejea kwa Mwenyezi Mungu kwa yale ayapendayo na kuyaridhi. Basi ule upole wake, na rehema zake, na huruma zake ndizo zilizo mpelekea kubishana kule kwa kutaraji kuwa asaa Mwenyezi Mungu akawaondolea adhabu watu wa Lut', na wao wapate kutubu na kurejea kwake.

76 Malaika wakasema: Ewe Ibrahim! Wachilia mbali haya majadiliano, na kuwatakiya rehema watu hawa. Kwani amri ya Mola wako Mlezi ya kuwaangamiza imekwisha kuja! Hapana budi kuwa adhabu itawashukia, na wala haitarudishwa kwa majadiliano au bila ya majadiliano.

77 Walipo kuja wajumbe wetu, hao Malaika, kwa Lut' kwa sura ya vijana wazuri, Lut' aliungulika na akauhika. Alihisi unyonge hana nguvu za kuwahami na hao watu wake, akawaonea dhiki kwa kuwaogopea ufisadi wa kaumu yake! Akasema: Hii leo ni siku ya karaha kubwa na machungu!

78 Watu wake wakajua kuwa wamekuja wale wageni, wakamwendea mbio mbio. Na kabla ya hayo ilikuwa kazi yao kufanya huo uchafu wao na kutenda maovu! Lut' akawaambia: Enyi watu wangu! Hawa binti zangu, waoeni. Hao ni safi zaidi kwenu kuliko kwenda kufanya uchafu kwa wanaume! Mwgopeni Mwenyezi Mungu, na jilindeni nafsi zenu na adhabu yake; na msinifedhehi na mkanidharaulisha kwa kuwavamia wageni wangu! Basi hivyo hamna kati yenu hata mtu mmoja mwenye rai iliyo sawa, mwenye akili iliyo ongoka, akakuziueni na maasi na akakukatazeni maovu?

79 Wakasema: Wajua vyema ewe Lut', kuwa sisi hatuna haki ya kuwaoa binti zako, wala hatuwataki. Na wewe hapana shaka unajua tukitakacho tulipo kujia kwa haraka.

80 Lut' akasema: Laiti ningeli kuwa nina nguvu au nina nguzo yenye nguvu ya kutegemea, msimamo wangu juu yenu ungeli kuwa mwengine, na ningeli weza kuwalinda wageni wangu nikakuziueni msiwafanye mambo mabaya.

81 Malaika wale wakamwambia, na wao ukweli wao ulikwisha dhihiri: Ewe Lut'! Usikhofu wala usihuzunike! Sisi ni wajumbe wa Mola wako Mlezi, wala si binaadamu kama tuonekanavyo kwako

- 82.** Basi ilipo fika amri yetu tuliigeuza nchi juu chini, na tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu ulio kamatana wa Motoni,⁸²
- 83.** Zilizo tiwa alama kwa Mola wako Mlezi. Na haya hayako mbali na wenye kudhulumu wengineo.⁸³
- 84.** Na kwa watu wa Madyana tuliwatumia ndugu yao Shua'ib. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye, wala msipunguze vipimo na mizani. Mimi nakuoneni mmo katika hali njema, nami nakukhofieni adhabu ya Siku kubwa hiyo itakayo kuzungukeni.⁸⁴
- 85.** Na enyi watu wangu! Timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu wala msiwakhini watu vitu vyao; wala msieneze uovu katika nchi mkafanya uharibifu.⁸⁵
- 86.** Alivyo kubakishieni Mwenyezi Mungu ndiyo bora kwa ajili yenu, ikiwa nyinyi ni Waumini. Wala mimi siye mlinzi wenu.⁸⁶
- 87.** Wakasema: Ewe Shua'ibu! Ni sala zako ndizo zinazo kuamrisha tuyaache waliyo kuwa wakiyaabudu baba zetu, au tuache kufanya tupendavyo katika mali zetu? Ama hakika wewe ni mstahamilivu kweli na mwongofu!⁸⁷
- 88.** Akasema: Enyi watu wangu! Mwaonaje ikiwa ninayo dalili wazi inayo tokana na Mola wangu Mlezi, na ikawa Yeye ameniruzuku riziki njema kutoka kwake? Wala mimi sipendi kukukhalifuni nikafanya yale ninayo kukatazeni. Sitaki ila kutengeneza kiasi ninavyo weza. Na sipati kuwezesha haya ila na Mwenyezi Mungu. Kwake

na kwa hawa kaumu yako. Wala wao hawa hawatakuifikishia shari yoyote ya kukuudhi au kukudhuru. Basi toka wewe na ahali zako usiku ukisha zaga. Mtoke mji huu, wala yeyote katika nyinyi asigeuke kutazama nyuma, asije akaona vitisho vya adhabu naye akasibiwa na shari yake! Lakini mkeo ambaye amekukhuni, yeye hatokuwa pamoja na watao toka nawe. Yeye lazima yampate yatao wapata hawa watu. Na miadi ya kuangamia kwao ni asubuhi, na miadi hiyo ni karibu. Basi usitie khofu.

82 Ulipo fika wakati wa adhabu tuliyo ikadiria na tukaitolea hukumu, tuliupindua mji ule walio kuwa wakiishi ndani kaumu Lut' juu chini. Na tukawanyesha mvua ya mawe ya udongo ulio okwa Motoni hata ukawa changarawe!

83 Wakawa wanaangukiwa na hayo mawe mfululizo kuwa ni adhabu inayo toka kwa Mola wako Mlezi, ewe Nabii! Na hayo si mbali kumfikilia kila mwenye kudhulumu katika kaumu yako.

84 Na kwa watu wa Madyana tulimtuma ndugu yao kwa nasaba na mapenzi na kuoneana huruma, Shua'ib. Aliwaambia: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu Mmoja peke yake. Nyinyi hamna anaye stahiki kuabudiwa isipo kwa Yeye. Wala msipunguze vipimo na mizani mnapo wauzia watu vitu vya kupimwa kwa pishi au kwa mizani. Hakika mimi nakuoneni ni watu wa kutarajiwa kheri kwa kumshukuru na kumt'ii Mwenyezi Mungu, na kuwapa watu haki zao kaamili. Na mimi nakukhofieni ikiwa hamtaishukuru kheri ya Mwenyezi Mungu na hamuitikii amri yake, isije ikakuteremkieni adhabu ya siku msio weza kuvikimbia vitisho vyake, kwa kuwa hivyo huwazinga wanao adhibiwa wasipate njia ya kusalimika. (*Tazama Maelezo 11:84*)

85 Enyi watu wangu! Toeni vipimo na mizani sawa na kwa uadilifu pale mnapo uza, wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye ujeuri na fisadi katika nchi kwa kwiba mali ya watu na kupokonya, au kuvamia wapita njia, mkifanya fisadi ndio chumo la maisha yenu.

86 Kidogo kinacho kuzidieni katika mali ya halali aliyo kuruzukuni Mwenyezi Mungu ni bora kwenu kuliko chungu ya mali mnapo yakusanya kwa njia ya haramu, ikiwa nyinyi kweli mnamuamini Mwenyezi Mungu, na mnaepuka aliyo kukatazeni. Basi jipimeni nafsi zenu, na mumuangalie Mola wenu Mlezi. Mimi si mlinzi wenu wa kuchunga vitendo vyenu na kukupimieni.

87 Wakasema kwa maskhara na kukejeli: Ewe Shua'ibu! Hivyo ni hizo sala zako ndizo zinazo kuamrisha kutushikilia tuache kuabudu masanamu waliyo kuwa wakiyaabudu baba zetu, na tuache kustarehe kutumia mali zetu kama tunavyoona wenyewe kuwa ni maslahi yetu? Hakika huo ndio mwisho wa upumbavu na utovu wa akili, wala haulingani na akili na raj njema tunazo kujua unazo; kwani wewe ni maarufu kwa ustahamilivu wako na uwongofu wako!

Yeye ninategemea, na kwake Yeye naelekea.⁸⁸

89. Na enyi watu wangu! Kukhalifiana nami kusikupelekeeni hata mkasibiwa kama walivyo sibiwa watu wa Nuhu, au watu wa Hud, au watu wa Saleh. Na watu wa Lut' si mbali nanyi.⁸⁹

90. Na ombeni msamaha kwa Mola wenu Mlezi, tena tubuni kwake. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye kurehemu na Mwenye upendo.⁹⁰

91. Wakasema: Ewe Shua'ibu! Mengi katika hayo unayo yasema hatuyafahamu. Na sisi tunakuona huna nguvu kwetu. Lau kuwa si jamaa zako tunge kupiga mawe, wala wewe si mtukufu kwetu.⁹¹

92. Akasema: Enyi watu wangu! Kwani jamaa zangu ni watukufu zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu? Na Yeye mmemueka nyuma ya migongo yenu! Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye kuyazunguka yote mnayo yatenda.⁹²

93. Na enyi watu wangu! Fanyeni mwezayo, na mimi pia ninafanya. Karibuni mtajua ni nani itakaye mfikia adhabu ya kumhizi, na nani aliye mwongo. Na ngojeni, mimi pia ninangoja pamoja nanyi.⁹³

94. Na ilipo fika amri yetu, tulimwoko Shua'ibu na wale walio amini pamoja naye kwa rehema yetu. Na ukelele uliwanyakua walio dhulumu, na wakapambaukiwa majumbani mwao wamekufa kifudufudi!⁹⁴

88 Yeye akasema: Enyi watu! Hebu nambieni, ikiwa mimi nina hoja iliyo wazi na ya yakini kutokana na Mola Mlezi wangu, naye akaniruzuku kwa fadhila yake riziki iliyo njema, je ingeli nifalia mimi nifiche aliyo niamrisha kukufikishieni, nako ni kuacha kuabudu masanamu, na kukutakeni mtimize vipimo na mizani, na muache kufanya uharibifu katika nchi? Na mimi si kama ninapenda kwenda kutenda haya ninayo kukatazeni, wala sitaki kwa mawaidha yangu, na nasaha zangu, na amri zangu, na makatazo yangu, ila kutengeneza kwa kadri ya ukomo wa uwezo wangu, na juhudi yangu, kama nilivyo jaaliwa. Wala sina uwezo wa kuifikilia haki ila kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na kuungwa mkono naye, na ninamtegemea Yeye peke yake. Na kwake Yeye tu ndio ninarejea.

89 Na enyi watu! Hizi khitilafu ziliopo baina yangu na nyinyi zisikupelekeeni kufanya inda na mkashikilia ukafiri, hata yakakupateni yaliyo wapata kaumu ya Nuhu, na kaumu ya Hud, na kaumu ya Saleh. Na wala zama na pahala pa kaumu Lut' na maangamizo yao si mbali nanyi! Basi zingatieni yasikusibuni yaliyo wasibu hao.

90 Na mtakeni Mwenyezi Mungu akusameheni madhambi yenu, na rejeeni kwake kwa majuto mkiomba maghira kila mtendapo dhambi. Hakika Mola wangu Mlezi ni mwingi wa rehema, ni mwenye mapenzi. Huwasamehe wenye kutubu, na anawapenda wenye kurejea kwake.

91 Wakasema: Ewe Shua'ibu! Mengi unayo yasema sisi hatuyafahamu! Na sisi tunakuhakikishia kuwa sisi tunakuona wewe dhaifu, huna nguvu zozote za kujitetea, wala kutukinaisha tukitaka kukutenda unayo yachukia. Na lau kuwa si kwa wema wetu kwa jamaa zako, kwani wao wanafuata dini yetu, tungeli kuulia mbali kwa kukupiga mawe. Na wewe si mtukufu kati yetu hata tukutukuze, na tukuhishimu, na tukukirimu na tuache kukuwa kwa mawe! Ni wema tunao wafanyia jamaa zako tu ndio unao tuzuia tusikuuwe.

92 Akasema Shua'ibu: Enyi watu wangu! Hivyo jamaa zangu ndio wanastahiki kufanyiwa wema kuliko Mwenyezi Mungu. Wao mnawakumbuka, na mkataka kunifanyia jamala mimi kwa ajili yao. Lakini Yeye mmemsahau na mkamfanya kama kitu kilicho tupiliwa mbali nyuma ya migongo yenu! Hakika Mola Mlezi wangu ni Mwenye kuyazunguka yote mnayo yafanya kwa kuyajua, hapana linalo fichikana kwake katika vitendo vyenu, na atakuhisabieni kwavyo hata ikiwa nyinyi mtasahau.

93 Enyi watu wangu! Tendeni mnayo weza nyinyi kuyatenda. Kama hamsikilizi nasaha zangu, mimi naendelea kushikilia kutenda kinyume na vitendo vyenu. Na hapo tutakuja jua ni nani kati yetu ataye fikiwa na adhabu ya kumfedhehi na kumdhalilisha, na ni nani kati yetu ni mwongo - mimi ninaye kuonyeni na adhabu, au nyinyi mnao nionya kunifukuza katika mji wenu? Ngojeeni nini litatokea, na mimi nangojea pamoja nanyi.

94 Ilipo kuja amri yetu ya kuwaadhibu na kuwaangamiza, tulimwoko Shua'ibu na walio amini pamoja

95. Kama kwamba hawakuwamo humo. Zingatia walivyo angamia watu wa Madyana, kama walivyo angamia watu wa Thamud!⁹⁵
96. Na hakika tulimtuma Musa pamoja na Ishara zetu na uthibitisho ulio wazi.⁹⁶
97. Kwa Firauni na waheshimiwa wake. Lakini wao walifuata amri ya Firauni, na amri ya Firauni haikuwa yenye uwongofu.⁹⁷
98. Siku ya Kiyama atawatangulia watu wake na atawaingiza Motoni. Na muingio muovu ulioje huo!⁹⁸
99. Nao wamefuatishiwa laana hapa duniani na Siku ya Kiyama. Ni mabaya yalioje watakayo pewa!⁹⁹
100. Hizi ni katika khabari za miji, tunakusimulia. Mengine ipo bado na mengine imefyekwa.¹⁰⁰
101. Na Sisi hatukuwadhulumu, lakini wao wenyewe wamejidhulumu. Na miungu yao waliyo kuwa wakiiomba badala ya Mwenyezi Mungu haikuwafaa kitu ilipo kuja amri ya Mola wako Mlezi. Na hiyo miungu haikuwazidishia ila maangamizo tu.¹⁰¹
102. Na ndio kama hivyo ndivyo inavyo kuwa Mola wako Mlezi anapo ikamata miji inapo kuwa imedhulumu. Hakika mkamoto wake ni mchungu na mkali.¹⁰²
103. Hakika katika haya ipo ishara kwa yule anaye ogopa adhabu ya Akhera. Hiyo

naye wasipate adhabu na maangamizo. Kuokoka kwao kulikuwa kutokana na rehema iliyo tokana nasi. Ukelele uliwatwaa watu wa Madyana, na tetemeko la kuteketeza, wakapambaukiwa wamekwisha jifia katika majumba yao, wamelala kifudifudi, hawatukusiki hata kidogo!

95 Mambo yakawishia, na athari zao zikapotea. Wakawa kama kwamba hawajapata kukaa katika majumba yao! Hali yao ikatamka ya kumzindua kila mwenye akili apate kuzingatia! Zingatia basi maangamizo ya Madyana, na vipi walivyo baidika na rehema ya Mwenyezi Mungu kama walivyo baidika watu wa Thamud kabla yao!

96 Na hakika tulimtuma Musa na tukamuunga mkono kwa miujiza yenye kuonyesha ukweli wake, na uthibitisho ulio wazi wenye nguvu juu ya nafsi.

97 Tulimtuma ende kwa Firauni na wakuu katika watu wake. Firauni akamkanya Musa na akawaamrisha watu wake wamfuata yeye Firauni katika ukafiri wake. Wakenda kinyume na amri ya Musa! Wala amri ya Firauni haikuwa ni nyoofu yenye matokea mema hata istahiki kufuatwa.

98 Siku ya Kiyama Firauni atawatangulia kaumu yake kama alivyo watangulia hapa duniani, na atawaingiza Motoni wakipenda wasipende, wataingia humo wakizigugumia adhabu zake! Na uovu ulioje wa maji yanayo tokota watayo kunywa humo kutafuta kuondoa kiu; maji hayo yatakatakata matumbo yao!

99 Na wao katika dunia hii iliwafuata laana ya Mwenyezi Mungu, na ya Malaika, na ya watu. Na Siku ya Kiyama kadhaalika itawafuata laana hiyo vile vile, kwani hiyo ndiyo zawadi yao. Zawadi hiyo ni ovu ya kuonyesha dhambi. Itasemwa : Ovu mno zawadi hii wapewao watu hawa!

100 Hadithi hio, ewe Nabii, ni baadhi ya khabari za miji tuliyo iteketeza. Tunakusimulia wewe upate kuwatolea mawaidha kwa khabari hizo watu wako, na utumaini kuwa Mwenyezi Mungu atakunusuru. Baadhi ya miji hiyo imekuwa kama mimea iliyo simama juu ya mashina yake ili waone yaliyo tokea, na baadhi yao imefutika athari yake kama mazao yaliyo kwisha vunwa.

101 Wala Sisi hatukuwadhulumu kwa vile tulivyo wateketeza; lakini wamejidhulumu wenyewe kwa kufuru zao, na kuacha kumuabudu Mwenyezi Mungu, na kuleta uharibifu katika nchi. Kwa hivyo miungu yao waliyo kuwa wakiiabudu badala ya Mwenyezi Mungu haikuweza kuwakinga na hilaki, wala haikuwafaa kitu ilipo kuja amri ya Mola wako Mlezi, ewe Nabii! Na kushikilia kwao kuabudu masanamu hakukuwazidishia ila hilaki na upotovu!

102 Na kuwateketeza kwa ukali kama huu, ewe Nabii, alivyo wateketeza Mola wako Mlezi kaumu ya Nuhu, na ya A'adi, na ya Thamud, na wengineo, ndivyo anavyo itwaa kwa nguvu miji inapo kuwa watu wake wanaingia katika dhulma kwa ukafiri na uharibifu! Hakika kuangamiza kwake Mwenyezi Mungu kuna nguvu, na kuna uchungu, na ukali kwa wenye kudhulumu.

ndiyo Siku itakayo kusanyiwa watu, na hiyo ndiyo Siku itakayo shuhudiwa.¹⁰³

104. Na Sisi hatuiakhirishi ila kwa muda unao hisabiwa.¹⁰⁴

105. Siku hiyo itakapo fika, hatosema hata mtu mmoja ila kwa idhini yake Mwenyezi Mungu. Kati yao watakuwamo waliomo mashakani na wenye furaha.¹⁰⁵

106. Ama wale wa mashakani hao watakuwamo Motoni wakiyayayatika na kukoroma.¹⁰⁶

107. Watadumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipo kuwa apendavyo Mola wako Mlezi. Hakika Mola wako Mlezi hutenda apendavyo.¹⁰⁷

108. Na ama wale walio bahatika, wao watakuwamo Peponi wakidumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipo kuwa apendavyo Mola wako Mlezi. Hicho ni kipawa kisio na ukomo.¹⁰⁸

109. Basi usiwe na shaka juu ya wanayo yaabudu hao. Hawaabudu ila kama walivyo abudu baba zao zamani. Na hakika Sisi tutawatimilizia fungu lao bila ya kupunguzwa.¹⁰⁹

110. Na kwa yakini tulimpa Musa Kitabu; zikazuka khitilafu ndani yake. Na lau kuwa si neno lilio kwisha tangulia kutoka kwa Mola wako Mlezi, bila ya shaka ingeli hukumiwa baina yao. Na hakika wao wamo katika shaka juu yake inayo wahangaisha.¹¹⁰

111. Na hakika Mola wako Mlezi atawatimilizia malipo ya vitendo vyao. Hakika Yeye

103 Hakika katika hadithi hizi yapo mawaidha yanayo faa kuzingatiwa na wenye kuyakinika kuwa kupo kufufuliwa, na kwa wenye kukhofu adhabu ya Siku ya Mwisho! Siku hiyo ndiyo Siku ya kukusanywa watu kwa ajili ya hisabu, na Siku hiyo itashuhudiwa na Malaika na watu pia.

104 Wala Sisi hatuiakhirishi ila kwa muda mfupi tuliyo kwisha uwekea kiwango. Na ingawa kwa nadhari ya watu itaonekana iko mbali, kwa Mwenyezi Mungu ni muda mchache tu.

105 Kikija kitisho chake mwanaadamu hatoweza kusema ila kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu. Kwani miongoni mwa watu wapo wenye mashaka, dhiki, wasio na bahati kwa kila namna ya shida watazo pata. Hao ndio makafiri. Na wengine wenye furaha, walio bahatika, kwa neema zinazo wangojea Akhera. Hao ndio Waumini.

106 Ama wale wenye mashaka mwisho wao ni Motoni. Kuvuta pumzi kwao kutakuwa ni kwa machungu makubwa, na mikoromo na kuyayatika, wanapo vuta pumzi na kutoa.

107 Watadumu Motoni muda wa kudumu mbingu na ardhi. Hawatotoka humo mpaka apendapo Mwenyezi Mungu, awaadhibu kwa adhabu namna nyengine! Ewe Nabii, Mwenyezi Mungu hutenda atakalo; hapana yeyote wa kumzuia.

108 Ama wale ambao Mwenyezi Mungu amewajaalia kuwa na bahati njema wataingia Peponi wadumu humo tangu mwanzo, mara baada ya kwisha hisabiwa. Huko hakuna mwisho. Isipo kuwa kikundi ambacho Mwenyezi Mungu anataka kukiakhirisha kisiingie pamoja na wale wa mwanzo - na hao ni wale Waumini walio fanya maasi. Hao watacheleweshwa Motoni kwa kadiri ya kupata adabu ya kuwasafisha wapate kuingia Peponi. Na Mwenyezi Mungu atawalipa hawa walio bahatika malipo bora kabisa ya kudumu, yasio na kasoro, wala yasio katika.

109 Ilivyo kuwa hali ya watu washirikina walio dhulumu katika dunia na akhera ni hiyo tuliyo kusimulia, ewe Nabii, basi usiwe na shaka yoyote juu ya mwisho wa hao katika kaumu yako wanao abudu masanamu pindi wakiendelea katika upotovu wao. Kwani hali yao ni hali ya baba zao walio watangulia, ambao khabari zao tumekusimulia. Wote hao ni washirikina. Na Sisi tutawatimilizia kwa ukafiri wao adhabu kaamili kwa kadiri ya makosa yao. Hawatapunguziwa hata chembe.

110 Na Sisi tunakuhakikishia, ewe Nabii, kwamba tulimpa Musa Taurati. Na watu wake baada yake wakakhitalifiana katika tafsiri yake na maana yake, kwa kufuata pumbao lao na matamania yao. Kila mmoja wao anataka kueleleza ifuate matamania yake. Wakafarikiana makundi mbali mbali. Wengi wao wakajitenga na Haki iliyo wajia. Na lau kuwa ahadi ya Mwenyezi Mungu haikutangulia kuwa itakhirishwa adhabu yao mpaka Siku ya Kiyama, ingeli wateremkia katika hii dunia yao hukumu ya Mwenyezi Mungu wakateketezwa wapotovu na wakaokoka walio na haki, kama yalivyo washukia wengineo, walio jiwa na ujumbe wakakhitalifiana katika kuufahamu baadae, na wakauguzwa, hata ikawa ni uzito kuifahamu kweli. Na hawa walio irithi Taurati wanababaika hawajui kweli iko wapi!

anayo khabari ya wayatendayo.¹¹¹

112. Basi, simama sawa sawa kama ulivyo amrisha, wewe na wale wanao elekea kwa Mwenyezi Mungu pamoja nawe; wala msikiuke mipaka. Hakika Yeye anayaona yote myatendayo.¹¹²

113. Wala msiwategemee wanao dhulumu, usije ukakuguseni Moto. Wala nyinyi hamna walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, wala tena hamtasaidiwa.¹¹³

114. Na shika Sala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizo karibu na mchana. Hakika mema huondoa maovu. Huu ni ukumbusho kwa wanao kumbuka.¹¹⁴

115. Na subiri, kwani Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa wanao fanya wema.¹¹⁵

116. Basi mbona hawakuwamo katika watu wa kabla yenu wenye vyeo na wasaa wanao kataza uharibifu katika nchi, isipo kuwa wachache tu, ambao ndio tulio waokoa? Na walio dhulumu walifuata starehe zao, na wakawa ni wakosefu.¹¹⁶

117. Wala hakuwa Mola wako Mlezi wa kuihiliki miji kwa dhulma tu na hali watu wake ni watenda mema.¹¹⁷

118. Na Mola wako Mlezi angeli penda ange wafanya watu wote wakawa umma mmoja. Lakini hawaachi kukhitalifiana,¹¹⁸

111 Hapana shaka yoyote kila kikundi katika hawa Mola wako Mlezi atawalipa jaza ya vitendo vyao. Hakika Yeye *Subhanahu* ni Mjuzi wa ukamilifu wa kubwa na dogo wanayo yatenda, ikiwa kheri na ikiwa shari. Na atamlipa kila mmoja wapo kwa mujibu alivyo tenda.

112 Ikiwa hii ndiyo hali ya kaumu zilizo jiwa na Kitabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, nao wakakhitalifiana kwacho na wakakitupa, basi jilazimishe kusimama sawa sawa wewe na Waumini walio pamoja nawe kuifuata Njia Iliyo Nyooka kama alivyo kuamrisha Mwenyezi Mungu. Wala msipindukie mipaka ya uadilifu kwa kupunguza, na kupuuza, na kuzidisha, kwa kuzikalifisha nafsi zenu kwa msilo liweza. Hakika Yeye *Subhanahu* ameyazunguka kwa ujuzi wake yote mnyo yatenda, na atakulipeni kwayo.

113 Wala msiwapende hata kidogo maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu walio zidhulumu nafsi zao na wapakindukia mipaka ya Mwenyezi Mungu. Wala msiwategemee, au mkapendezewa na mwendo wao, na kwa kumili huko mkastahiki adhabu ya Moto, na msimpatye yeyote wa kuwatetea. Mwisho wenu mtakuwa hamtanusuriwa kwa maadui zenu kwa kuwa Mwenyezi Mungu atakutupeni na kwa kuwa nyinyi mnamtegemea adui yake!

114 Ewe Nabii! Timiza Sala kwa ukamilifu katika ncha mbili za mchana, na nyakati mbali mbali za usiku. Kwani Sala husafisha nafsi na hushinda katika kung'oa shari, na hufuta athari ya maovu ambayo mwanaadamu shida kuepukana nayo! Hayo uliyo amrisha, ewe Nabii, katika uwongofu wa kheri ni mawaidha ya kuwanufaisha wale ambao walio tayari kuyakubali, ambao kwamba wanamkumbuka Mola wao Mlezi, wala hawamsahau.

115 Ewe Nabii! Vumilia mashaka ya haya tunayo kuamrisha, na yatimize vilivyo. Mwenyezi Mungu atakulipa malipo makubwa. Kwani kwake Yeye hayapotei malipo ya watendao mema kwa mujibu wa vitendo vyao.

116 Ilikuwa inapasa katika kaumu zilizo tangulia na tukaziteketeza kwa dhulma zao, wawepo jamaa kati yao wenye kusikilizwa kauli yao, na wenye vyeo katika dini na akili, wawakanye wenzi wao waache uharibifu katika nchi, ili wasalimike na adhabu iliyo wateremkia. Lakini hayakuwa hayo. Yaliyo tokea ni kuwa walikuwapo Waumini wachache wasio sikilizwa rai zao wala uwongozi wao. Hao Mwenyezi Mungu aliwaokoa pamoja na Mitume wao wakati ule walipo shikilia wenye kudhulumu wenye inda kung'ang'anilia yale maisha ya anasa na fisadi waliyo yazoea. Hayo yakawa ni pingamizi wasiweze kunafiika na wito wa Haki na kheri, na kwa kukhiari kwao njia hiyo wakazama katika madhambi na vitendo viovu. Basi Mwenyezi Mungu akawahiliki kwa mujibu wa mwendo wake wa maumbile.

117 Wala sio mwendo wake Mwenyezi Mungu, wala sio uadilifu wake wa maumbile, kuudhulumu umma wowote akauteketeza nao unashikamana na Haki, unafuata mwendo bora, unatenda yanao wafaa wao na wenginewe.

118 Ewe Nabii! Lau kuwa Mola wako Mlezi angeli penda angeli wafanya watu wote wafuate dini moja, wakimt'ii Mwenyezi Mungu kwa ut'iifu wa maumbile, kama Malaika. Na ulimwengu ungeli kuwa sio ulimwengu huu. Lakini Yeye *Subhanahu* hakutaka hayo, bali amewaacha waweze kuchagua wenyewe.

119. Isipo kuwa wale ambao Mola wako Mlezi amewarehemu; na kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu amewaumba. Na litatimia neno la Mola wako Mlezi: Kweli kweli nitaijaza Jahannam kwa majini na watu pamoja.¹¹⁹

120. Na yote tunayo kusimulia katika khabari za Mitume ni ya kukupa nguvu moyo wako. Na katika haya imekujia haki na mawaidha na ukumbusho kwa Waumini.¹²⁰

121. Na waambie wale wasio amini: Fanyeni muwezavyo, nasi pia tunafanya.¹²¹

122. Na ngojeni, na sisi tunangoja.¹²²

123. Na ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyo fichikana katika ardhi na mbingu, na mambo yote yatarejezwa kwake. Basi muabudu Yeye na umtegemee Yeye. Na Mola wako Mlezi haghafiliki na yale mnayo yatenda.¹²³

Basi hawaachi kukhitalifiana katika kila kitu, hata katika misingi ya imani, kama kumuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya Mwisho - mambo ambayo haifai kukhitalifiana kwayo. Wao hufuata nyoyo zao, na matamaniao yao, na fikra zao, kila kikundi kimeshikilia kwa nguvu rai ile ile walio kutana nayo kwa baba zao!

119 Lakini wale Mwenyezi Mungu alio warehemu kwa kusalimika kwao kwa walivyo jaaliwa, hao wameridhia hukumu ya Mwenyezi Mungu juu yao, wakawaamini Mitume wake wote, na Vitabu vyake vyote, na Siku ya Mwisho. Na kwa namna hivi ilivyo pita hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika mpango wa huu ulimwengu ndivyo alivyo waambia *Subhanahu* kwa kuwaweka tayari kuwateua na kuwavusha na hizo khitalafu, ili aweke tayari panapo stahiki thawabu na adhabu. Kwa hivyo ahadi ya Mola wako Mlezi itatimia ya kwamba hapana budi kuwa ataijaza Jahannamu kwa wafuasi wa Iblis miongoni mwa majini na watu.

120 Ewe Nabii! Tunakusimulia kila namna ya khabari ya Mitume walio pita pamoja na kaumu zao kwa ajili ya kukupa nguvu wewe uweze kubeba mashaka ya Utume. Na katika khabari hizi yamekujia maelezo ya haki unayo ilingania mfano walivyo lingania Mitume walio kutangulia, nayo ni Tawhidi ya kuwa Mwenyezi Mungu ni Mpweke, na kuepuka yale ambayo yanamkasirisha, kama yalivyo wajia mawaidha na mazingatio yanayo wanufaisha Waumini, ili wazidi imani yao, na wanao jitayarisha kwa imani ili waifanyie haraka hiyo imani.

121 Ewe Nabii! Waambie hao wanao shikilia inadi na ukafiri: Tendeni kama mnavyo weza kuupiga vita Uislamu na kuwaudhi Waumini. Sisi tunaendelea na njia yetu, na tumethibiti katika a'mali yetu.

122 Na yangojeni hayo mnayo yangojea, na sisi kadhaalika tunangojea ahadi ya Mwenyezi Mungu, kuwa wito wetu utashinda na tutawashinda maadui zake.

123 Ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kujua yaliyo ya ghaibu katika mbingu na ardhi. Anayajua yatakayo kufikieni, na yatakayo tufikia sisi. Ni kwake Yeye tu yanarejea mambo yote kuendeshwa. Ilivyo kuwa mambo ni hivyo, basi muabudu Mola wako Mlezi peke yake, na mtegemee Yeye, wala usimwogope yeyote isipo kuwa Yeye. Na Mola wako Mlezi haghafiliki kabisa na yote myatendayo, enyi Waumini na makafiri. Na kila mmoja atalipwa hapa duniani na Akhera kwa mujibu anavyo stahiki.

Sura 12 - Yusuf

Utangulizi

Sura hii ni ya Makka, na Aya zake ni mia na kumi na moja. Ndani yake Mwenyezi Mungu amesimulia hadithi ya Yusuf katika Aya tisiini na nane, na ameitangulizia kwa Aya tatu alizo taja ndani yake huu ufunuo alio mteremshia Muhammad, rehema za Mwenyezi Mungu na amani zishuke juu yake. Na ameuita ufunuo huu katika Aya ya kwanza: Kitabu kinacho bainisha. Na katika Aya ya pili akauita: Qur'ani kwa Kiarabu, kuwa ni kuashiria kwamba ni haki yake uhifadhiwe kwa maandishi na katika vifua vya watu vile vile. Kisha katika Aya ya tatu akataja kuwa ufunuo huu umekusanya simulizi nzuri kabisa, na ukataja kuwa Nabii Muhammad hakuwa akiyajua hayo kabla hakuteremshiwa huo Wahyi (ufunuo). Na hiyo ni dalili kuwa haya yanatoka kwa Mwenyezi Mungu. Na kisa hichi na Sura hii imemalizikia kwa kutilia mkazo yaliyo anzia. Na akamuelekeza Nabii mnamo Aya kumi azingatie kuwa masimulizi haya ni katika khabari za ghaibu, ambazo yeye Nabii, *Salla Llahu alayhi wasallama*, hakuwa akizijua, na kuzijua ukweli wake zilivyo, kabla ya kuteremshiwa Wahyi. Wala yeye hakuwa pamoja na hao ndugu zake Yusuf walipo kuwa wakipanga mipango yao, na wakiunda njama zao za shari kumuundia ndugu yao kwa baba. Kisha Qur'ani inamwambia Mtume kuwa inda na husda huwapelekea watu wengi kuingia ukafirini. Na kwamba pupa yake Mtume s.a.w. kuwa waamini wengi wao haitomfalia kitu, lakini Qur'ani inampoza kwa hayo kwa kuwa yeye hataki ujira, ila ni kuwa yeye anawaletoa Qur'ani iwe ni uwongofu na ukumbusho kwa watu wote. Na mwisho wa Sura inaashiria Mitume ambao hadithi zao zimesimuliwa, na ukasimuliwa msimamo wa kaumu zao, na vipi mwisho walivyo washinda makafiri wakosefu. Na katika hadithi hizi za Manabii pana mazingatio kwa wenye akili. Hakika hii Qur'ani inayo simulia masimulio haya na mengineyo si kitu cha kutungwa tu na kuzuliwa kuwa kinatoka kwa Mwenyezi Mungu kwa uwongo. Hakika hii ni haki na kweli tupu, na hichi ni Kitabu kinacho sadikisha Vitabu sahihi vilivyo toka mbinguni, na ni uwongofu, na rehema kwa watu wanao zingatia na wakaamini.

Linalo onekana wazi katika sifa za Sura hii ni kuwa kimesimuliwa kisa cha Yusuf kwa ukamilifu wake. Na pia imeonekana kuwa katika ule ule ukoo mmoja upo uhasidi ulio enea na pia katika baadhi yao yapo mapenzi. Husda ya wana wa Yaaqub iliwapelekea kumtumbukiza ndugu yao kisimani. Lakini Mwenyezi Mungu alimlinda na vitimbi vyao, kama alivyo mkinga na matamano ya mke wa Mheshimiwa pale Yusuf alipo fikilia utuuzima nyumbani kwa Mheshimiwa. Mwenyezi Mungu akamweka vizuri katika nchi ya Misri, na akamjaalia kuwa nchi hiyo iwe makimbilio (mategemeo) ya wale walio mpangia njama za kumdhuru. Basi ni hivyo shani yake *Subhanahu wa Taa'la* kwa Manabii wake na vipenzi vyake. Huwanusuru dhidi ya maadui zao, na huwathibitisha na kuwaweka vyema katika ardhi maadamu wanaishika Haki na wanaamini, na wanaishikilia kamba ya Mwenyezi Mungu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Raa. Hizi ni Aya za Kitabu kinacho bainisha.¹
2. Hakika Sisi tumeiteremsha Qur’ani kwa Kiarabu ili mpate kuzingatia.²
3. Sisi tunasimulia simulizi nzuri kwa kukufunulia Qur’ani hii. Na ijapo kuwa kabla ya haya ulikuwa miongoni mwa wasio jua.³
4. Yusuf alipo mwambia baba yake: Ewe babaangu! Hakika mimi nimeota nyota kumi na moja, na jua, na mwezi. Nimeota zikinisujudia.⁴
5. (Baba) akasema: Ewe mwanangu! Usiwasimulie nduguzo ndoto yako, wasije wakakufanyia vitimbi. Hakika Shet’ani ni adui aliye dhaahiri kwa mwanaadamu.⁵
6. Na kadhaalika Mola wako Mlezi atakuteuwa na atakufundisha tafsiri ya mambo. Na atatimiza neema zake juu yako na juu ya ukoo wa Yaa’qub, kama alivyo watimiza hapo zamani baba zako Ibrahim na Is-haq. Hakika Mola wako Mlezi ni Mjuzi Mwenye hikima.⁶
7. Kwa yakini katika Yusuf na nduguze ziko ishara kwa wanao uliza.⁷
8. Pale walipo sema: Hakika Yusuf na nduguye wanapendwa zaidi na baba yetu kuliko sisi, hali sisi ni kikundi chenye nguvu. Hakika baba yetu yumo katika upotofu wa dhaahiri.⁸
9. Muuweni Yusuf, au mtupeni nchi mbali ili uso wa baba yenu ukuelekeeni nyinyi. Na baada ya haya mtakuwa watu wema.⁹

1 Alif, Lam, Raa. Hizi harufi na mfano wake, zinazo fanya maneno yenu, enyi Waarabu, ndizo hizo zinazo fanya Aya za hichi Kitabu, ambacho ni muujiza unao waemea watu kuuiga. Muujiza ulio wazi unao fafanua kwa kila mwenye kutafuta uwongozi ndani yake, na uwongofu. Na kwa hizi harufi za kutamkika zikasikilizana sauti yake wanazinduliwa watu watanabahi. Basi wasikilize, ijapo kuwa waliwafikiana kuwa wasisikilize.

2 Hakika Sisi tumemteremshia Mtume wetu haya maneno kwa lugha yenu ya Kiarabu yasomwe na yahifadhiwe, ili muyafahamu, na muwafikishie watu wote.

3 Sisi tunakusimulia, ewe Nabii, visa vizuri kabisa kwa kukufunulia Kitabu hichi. Na kabla ya haya ulikuwa umeghafilika nayo, huyajui, haya, wala mawaidha yaliomo ndani yake, na Aya zake zilizo wazi.

4 Katika visa hivi, ewe Nabii, kipo hichi kisa cha Yusuf, pale alipo mwambia baba yake: Ewe babaangu! Hakika mimi nimeona usingizini nyota hidaa’shara, na jua, na mwezi. Nimeona vyote hivyo vikininyenyekea, vikisujudu mbele yangu. (*Tazama Maelezo 12:4*)

5 Baba yake akamwambia: Ewe mwanangu! Usiwasimulie nduguzo ndoto yako hii. Itakuja watia husda katika nyoyo zao, na Shetani atawachochea wazue njama kukupinga. Watakuja kufanyia hila na vitimbi! Hakika Shetani ni adui wazi wa binaadamu!

6 Kama ulivyo jiona katika ndoto kuwa ni bwana wa kut’iwa, mwenye cheo na madaraka, basi Mola wako Mlezi atakuteuwa na atakukhitari, akufunze kufasiri ndoto, kwa kukupa Unabii na Utume, kama hapo zamani, kabla ya baba yako, Yaa’qub, alivyo wafanyia baba zako, Ibrahim na Is-haq. Hakika Mola wako Mlezi ni mwingi wa hikima, basi hakosei. Ni mwingi wa ujuzi, basi humteuwa katika waja wake anaye mjua kuwa anastahili kuteuliwa.

7 Hakika katika kisa cha Yusuf na nduguze zipo dalili na mazingatio kwa waulizao, wenye kutaka kujua.

8 Walipo semezana nduguze Yusuf kwa baba: Bila ya shaka Yusuf na nduguye kwa baba na mama wanapendwa zaidi na baba yetu kuliko sisi. Na sisi ni kikundi chenye nguvu, chenye kumfaa yeye zaidi kuliko wao! Hakika baba yetu kwa kumfadhilisha Yusuf na nduguye kuliko sisi yumo makosani, na yuko mbali na haki. Yalio sawa yapo wazi yanaonekana.

9 Muuweni Yusuf, au mtupeni nchi iliyo mbali na baba yenu, asiyo weza kuifikia. Yatakuwafikieni nyinyi tu mapenzi ya baba yenu, na atakuelekeeni nyinyi tu. Na baada ya kumtenga Yusuf naye kwa kumuwa au kumhamisha mtakuwa watu wema. Kwani Mwenyezi Mungu atakubali toba yenu, na baba yenu

10. Akasema msemaji kati yao: Msimuuwe Yusuf. Lakini mtumbukizeni ndani ya kisima. Wasafiri watakuja mwokota; kama nyinyi mna sharti ya kufanya jambo.¹⁰

11. Wakasema: Ewe baba yetu! Una nini hata hutuamini kwa Yusuf? Na hakika sisi ni wenye kumtakia kheri!¹¹

12. Mpeleke kesho pamoja nasi, ale kwa furaha na acheze; na bila ya shaka sisi tutamhifadhi.¹²

13. Akasem: Kwa hakika inanihuzunisha kwamba nyinyi mwende naye, na ninaogopa asije mbwa mwitu akamla nanyi mmeghafilika naye.¹³

14. Wakasema: Ikiwa mbwa mwitu atamla na hali sisi ni kundi lenye nguvu kabisa, basi bila ya shaka sisi tutakuwa khasarani.¹⁴

15. Basi walipo mchukua na wakakubaliana wamtumbukize ndani ya kisima, tulimfunulia Yusuf: Hapana shaka yoyote utakuja waambia kwa jambo lao hili, na wala wao hawatambui.¹⁵

16. Wakaja kwa baba yao usiku wakilia.¹⁶

17. Wakasema: Ewe baba yetu! Hakika tulikwenda kushindana na tukamwacha Yusuf penye vitu vyetu. Basi mbwa mwitu akamla. Lakini wewe hutuamini ijapo kuwa tunasema kweli.¹⁷

18. Wakaja na kanzu yake ina damu ya uwongo. Akasema: Bali nafsi zenu zimekushawishini kutenda kitendo. Lakini subira ni njema; na Mwenyezi Mungu ndiye wa kuombwa msaada kwa haya mnayo yaeleza.¹⁸

atapokea udhuru wenu.

10 Mmoja wao katika wasemaji alisema: Msimuuwe Yusuf. Hayo ni makosa makubwa. Lakini mtupeni asipo onekana ndani ya kisima, baadhi ya wapita njia watakuja mwokota, watapo tumbukiza ndoo yao kisimani. Hao watakwenda naye pahala pambali nanyi na baba yenu vile vile. Haya ikiwa nyinyi mna lazima mumpelkeke mbali na mtimize kwa kitendo hayo mtakayo.

11 Baada ya kuwafikiana kumbaidisha Yusuf (kumpeleka mbali) walisema: Ewe baba yetu! Nini kinacho kutia shaka nasi hata unamtenga Yusuf nasi, wala huoni pana usalama anapo kuwa nasi? Sisi tunakuhakikishia kuwa sisi tunampenda, na tunamwonea huruma, na tunamtakia kheri, na tunamwongoza kwenye kheri. Hapati kwetu isipo kuwa mahaba, na nasiha safi kabisa.

12 Mwache ende nasi kesho machungani. Atastarehe kwa kula vyakula vizuri, atacheza na atafurahi. Na sisi kwa yakini tuna hima ya kumhifadhi kumkinga na madhara yoyote.

13 Mzee akasema: Hakika mimi naona huzuni mkiondoka naye, akawa mbali nami. Na nina khofu nikikuaminini asije akaliwa na mbwa mwitu na nyinyi mmeghafilika naye.

14 Wakasema: Tunakuapia, akiliwa na mbwa, na hali sisi ni kundi lenye nguvu, basi itakuwa ni fedheha na khasara kwetu! Likitokea hilo unalo liogopa basi sisi tutakuwa tumekhasiri kila linalo pasa kulishughulikia, na kuwa lisitokee. Basi tuwa kwa hayo! Hatutadharau kumlinda, ikiwa hivyo itakuwa tunajipelekea wenyewe kupotea na kupuuzwa.

15 Walipo kwenda naye mbali na baba yake, na wakakubaliana rai yao ya kumtumbukiza ndani ya kisima, walifanya hayo waliyo yaazimia. Sisi tukamtia moyoni mwake Yusuf atulie, na awe na imani ya Mwenyezi Mungu, kuwa bila ya shaka atakuja waeleza haya mambo yao waliyo yapanga na wakayatenda, na wala wao wenyewe hawajui hapo utapo waambia kwamba wewe ndiye Yusuf waliye mfanyia vitimbi, na wakadhani wamekwisha mmaliza na wameepukana naye!

16 Walirejea kwa baba yao usiku, wakijitia huzuni, na kupiga makelele kwa kilio!

17 Wakasema: Ewe baba yetu! Sisi tulikwenda kushindana kupiga mishale na kwenda mbio, na tukamwacha Yusuf kwenye vitu vyetu avilinde. Mbwa mwitu akamla, na sisi tuko mbali tumeshughulika na mashindano! Na wewe hutusadiki tunayo yasema, ijapokuwa tunasema haki na kweli!

18 Wakaileta kanzu yake nayo ina damu, ati kuwa ni ushahidi wa yale madai yao ya kuwa ile ni damu ya Yusuf, apate kusadiki baba yao! Walakini yeye alisema: Hakika huyo mbwa mwitu hakumla kama mnavyo singizia, bali nafsi zenu zimekupelekeeni kufanya jambo kubwa, na mkalitimiza! Langu mimi

19. Ukafika msafara, wakamtuma mchota maji wao, naye akatumbukiza ndoo yake. Alisema: Kheri Inshallah! Huyu hapa mvulana! Wakamficha ili kumfanya ni bidhaa. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa wanayo yatenda.¹⁹

20. Na wakamuza kwa thamani duni, kwa akali ya pesa. Wala hawakuwa na haja naye.²⁰

21. Na yule aliye mnunua huko Misri alimwambia mkewe: Mtengenezee makaazi ya hishima huyu; huenda akatufaa au tukamfanya mwenetu. Na kama hivyo tulimweka Yusuf katika nchi ili tumfundishe kufasiri mambo. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kushinda katika jambo lake, lakini watu wengi hawajui.²¹

22. Na alipo fikilia utu uzima tulimpa hukumu na ilimu. Na kama hivi tunawalipa wanao tenda mema.²²

23. Na yule bibi wa nyumba aliyo kuwamo Yusuf alimtamani kinyume cha nafsi yake, na akafunga milango. Akamwambia: Njoo! Yusuf akasema: Audhubillahi! Najikinga na Mwenyezi Mungu. Huyu bwana wangu kaniweka maskani nzuri, na hakika wenye kudhulumu hawatengenekewi.²³

24. Na hakika yule mwanamke alimtamani, na Yusuf angeli mtamani lau kuwa hakuona ishara ya Mola wake Mlezi. Hayo hivyo ni kwa ajili tumuepushe na uovu na uchafu. Hakika yeye alikuwa katika waja wetu walio safishwa.²⁴

ni kusubiri subira njema isiyo legalega kwa mliyo nikutisha. Na Mwenyezi Mungu pekee ndiye anaye takiwa msaada kwa huo upotovu mlio uzua na mnao udai.

19 Wakaja watu upande ule wa kisima katika msafara wao wa kwendea Misri. Wakamtuma mtu kati yao wa kuchota maji kisimani awalettee. Akatumbukiza ndoo yake, akiivuta na Yusuf kang'ang'anilia! Yule mchota maji akapiga kelele za furaha: Kheri! Kheri gani hii na furaha! Huyu ni kijana! Wakamficha katika vitu vyao, wakamfanya ni bidhaa ya biashara! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyazunguka yote wayatendayo kwa ujuzi wake.

20 Wakamuza Misri kwa bei ya chini kabisa, si kiasi chake! Thamani yake ilikuwa ni pesa chache tu! Wala hawakuwa wakimtakia Yusuf thamani kubwa, kwa kukhofia wasije watu wake wakamkuta wakamtambua, na wakawapokonya Yusuf.

21 Yule aliye mnunua kule Misri alimwambia mkewe: Mfanyie wema huyu, na umhishimu, ili makao yake hapa nasi yawe mazuri. Huenda akatufaa, au tukamfanya kuwa ni mwenetu. Kama yalivyo kuwa makaazi yake ni mazuri na ya hishima, basi kadhaalika tulimjaalia Yusuf katika nchi ya Misri cheo kingine kikubwa, ili atekeleze uadilifu na mipango mizuri, na ili tumfunze kufasiri mambo na ndoto, ajue yatakayo kuwa kabla hayajawa, ili awe tayari kuyakabili! Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kutimiza kila jambo alitakalo. Kabisa haemewi na kitu. Lakini watu wengi hawajui siri ya hikima yake, na undani wa mipango yake.

22 Na Yusuf alipo timia ukomo wa nguvu zake tukampa hukumu yenye kusibu, na ilimu yenye kufaa. Na kama malipo haya tuliyo mpa yeye kwa wema wake, ndio tunavyo wapa wote walio wema kwa vitendo vyao vyema.

23 Na yule bibi aliye kuwa Yusuf anakaa nyumbani kwake, naye anamjua madaraka yake, alitaka kumghuri aache mwendo wake ulio safi. Akawa anajipitisha pitisha mbele yake kuonyesha uzuri wake, na kujitamanisha kwake. Hata mwisho akamfungia milango, na akamwambia: Njoo kwangu, nimejitoa kwako! Yusuf akasema: Mimi najilinda kwa Mwenyezi Mungu, aniepushe na hiyo shari! Na vipi nifanye uchafu huo nawe, na mumeo mheshimiwa ni bwana wangu aliye niweka bora ya makamo? Hakika hawafuzu wanao wadhulumu watu kwa udanganyifu na khiana, wakajitia wenyewe katika maasi ya uzinzi!

24 Na yule bibi aliazimia aingiane naye, na nafsi ya Yusuf ilimvutia kwake, lau kuwa hakuiona nuru ya Mwenyezi Mungu ya haki imezagaa mbele ya macho yake. Basi hakuufuata mvutio wa nafsi, na akayashinda matamanio, na akajizuiliana maasi na khiana. Akathibiti juu ya usafi na kutakasika kwake. Ndio hivi tulivyo mthibitisha Yusuf kwenye usafi na kutakasika, ili tumuepushe na uovu wa khiana na maasi ya uzinzi. Hakika yeye ni miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu walio itakasa dini yao kwa

25. Na wote wawili wakakimbilia mlangoni, na mwanamke akairarua kanzu yake Yusuf kwa nyuma. Na wakamkuta bwana wake mlangoni. Mwanamke akasema: Hapana malipo ya mwenye kutaka kumfanyia maovu mkeo isipo kuwa kufungwa au kupewa adhabu chungu.²⁵

26. Yusuf akasema: Yeye ndiye aliye nitaka bila ya mimi kumtaka. Na shahidi aliye kuwa katika jamaa za mwanamke alisema: Ikiwa kanzu yake imechanwa mbele basi mwanamke amesema kweli, naye Yusuf ni katika waongo.²⁶

27. Na ikiwa kanzu yake imechanwa nyuma, basi mwanamke amesema uwongo, naye Yusuf ni katika wakweli.²⁷

28. Basi yule bwana alipoona kanzu yake imechanwa kwa nyuma, alisema: Hakika haya ni katika vitimbi vyenu wanawake. Bila ya shaka vitimbi vyenu ni vikuu.²⁸

29. Yusuf! Wachilia mbali haya. Na wewe, mwanamke, omba msamaha kwa dhambi zako. Kwa hakika wewe ni katika walio fanya makosa.²⁹

30. Na wanawake wa mjini wakawa wanasema: Mke wa Mheshimiwa anamtamani mtumishi wake ! Hakika amesalitika kwa mapenzi. Sisi hakika tunamwona yumo katika upotovu ulio dhaahiri.³⁰

31. Alipo sikia yule bibi masengenyo yao aliwaita, na akawawekea matakia ya kuegemea, na akampa kila mmoja wao kisu. Akamwambia Yusuf: Tokeza mbele yao. Basi walipo mwona waliona ni kitu kikubwa kabisa, na wakajikata mikono yao. Wakasema: *Hasha Lillahi!* Huyu si mwanaadamu. Hakuwa huyu ila ni Malaika mtukufu.³¹

Mwenyezi Mungu.

25 Yusuf akakimbilia mlangoni kutaka kutoka, na yule bibi naye akapiga mbio amtangulie ili amzuie kutoka. Akaivuta kanzu yake kwa nyuma ili kumzuia, akaichana. Hapo wakapambana na mume wa yule bibi mlangoni! Yule bibi akasema kumchongea Yusuf: Hapana malipo ya mwenye kutaka kumfanya mkeo mambo mabaya ila atiwe gerezani, au akutishwe adhabu chungu!

26 Yusuf akasema kujitetea: Ni yeye ndiye aliyenitaka, na akajaribu kunikhadaa! Ikawa ni kusutana. Alikata hukumu mmojapo katika jamaa zake mwenyewe yule mwanamke kwa kusema: Ikiwa kanzu yake imechanwa mbele, basi huyu bibi kasema kweli katika madai yake, na huyu kijana ni mwongo kwa aliye yasema.

27 Na ikiwa kanzu yake imechanwa nyuma, basi huyu mwanamke kasema uwongo, na kijana ni mkweli kwa aliye yasema.

28 Mume alipoona kuwa kanzu ya Yusuf imechanwa mgongoni alimwambia mkewe: Huku kumtuhumu kwako kijana kwa yaliyo tokea na hali yeye hana makosa, ni katika vitimbi vyenu, enyi wanawake. Hakika vitimbi vyenu ni vikuu mno!

29 Ewe Yusuf wachilia mbali mambo haya, na wewe yafiche wala usiyaseme. Na wewe, mwanamke, omba maghfira kwa dhambi yako. Hapana shaka kuwa wewe ni katika wenye dhambi, wenye kuyakusudia makosa, na kutenda maasi, na kuwasingizia wengine uasi wasio ufanya!

30 Khabari zikawafikia baadhi ya wanawake wa mjini, wakazungumza wakisema: Mke wa Mheshimiwa anamzaini mtumishi wake na anamkhadaa amkubalie anayo yataka kwake! Ama kweli amesalitika kwa mahaba hata hajitambui! Hakika sisi tunaamini kuwa kwa mwendo wake huu ameingia kwenye upotovu na makosa yaliyo wazi.

31 Yule bibi alipo yasikia masengenyo yao wale wanawake na kuwa wanamsema kwa vibaya, aliwaalika nyumbani kwake na akawapangia matakia na mito ya kuegemea, na akampa kila mmoja wao kisu, baada ya kwisha hudhuria na wakakaa wakiegemea. Akawaletea chakula na visu vya kulia. Akamwambia Yusuf: Hebu watokee! Alipotokeza wakamwona walistaajabu. Uzuri wake ulio pita mpaka uliawatwaa wasijitambue, wakawa wanajikata mikono yao jinsi ya kushtuka kwao, na huku wanadhani wanakata chakula! Wakasema kwa mastaajabu na kushituka: *Hasha Lillahi!* Mungu apishe mbali! Huyu tunaye mwona si binaadamu! Hapana binaadamu mwenye uzuri namna hii, na mwenye jamali kama hivi, na

32. Yule bibi aksema: Huyu basi ndiye huyo mliye nilaumia! Na kweli mimi nilimta naye akakataa. Na akitofanya ninayo muamrisha basi hapana shaka atafungwa gerezani, na atakuwa miongoni mwa walio chini kabisa.³²

33. Yusuf akasema: Ee Mola Mlezi wangu! Nastahabu kifungo kuliko haya anayo niitia. Na usipo nondoshea vitimbi vya wanawake mimi nitamili kwao, na nitakuwa katika wajinga.³³

34. Basi Mola wake Mlezi akamwitikia, na akamwondoshea vitimbi vyao. Hakika Yeye ni Msikizi Mjuzi.³⁴

35. Basi ikawadhihirikia baada ya kuona Ishara kuwa wamfungue kwa muda.³⁵

36. Wakaingia gerezani pamoja naye vijana wawili. Mmoja wao akasema: Hakika mimi nimeota nakamua mvinyo. Na mwingine akasema: Mimi nimeota nimebeba mikate juu ya kichwa changu, na ndege wanaila. Hebu tuambie tafsiri yake, kwani sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.³⁶

37. Akasema: Hakitakufikilieni chakula mtakacho pewa ila nitakwambieni hakika yake kabla hakijakufikieni. Haya ni katika yale aliyo nifundisha Mola wangu Mlezi. Hakika mimi nimeacha mila ya watu wasio muamini Mwenyezi Mungu, na wakawa hawaiamini Akhera.³⁷

38. Na nimefuata mila ya baba zangu, Ibrahim, na Is-haq, na Yaa'qub. Hatuna haki ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote. Hiyo ni katika fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yetu na juu ya watu; lakini watu wengi hawashukuru.³⁸

usafi kama huu, na kunyooka kama huku! Huyu ni Malaika tu, mwenye uzuri huu, na sifa hizi zililo timia! 32 Tena mke wa Mheshimiwa alisema kufuatiliza maneno yao: Huyu kijana ambaye uzuri wake umekuzugeni na ukakuemeeni hata yakatokea yaliyo tokea ndiye ambaye nyinyi mliye nilaumia kwa ajili yake! Na mimi kweli nilimta, na nikafanya juhudi kumghuri anikubalie, naye akajizua na akakataa. Kama kwamba vile anavyo kataa ndio anazidi kumtia hamu yule mwanamke! Akasema mwanamke: Na mimi naapa! Kama hafanyi ninayo muamrisha atapata adhabu ya kifungo, na atakuwa katika madhalili wenye kudharauliwa!

33 Yusuf akasema naye alisikia vile vitishio, na akasikia kwa wale wanawake nasiha ya kuwa amkubalie, akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nakhiari kifungo kuliko hayo anayo nitakia huyu mwanamke. Kwani hayo ni kukuasi Wewe. Na kama Wewe hunikingi na shari ya vitimbi vyao na hila zao nitakuja wakubalia, na nitakuwa miongoni mwa wajinga walio potea.

34 Mwenyezi Mungu akamwitikia, na akamuepusha na shari ya vitimbi vyao. Hakika Yeye peke yake ndiye Mwenye kusikia maombi ya wenye kukimbilia kwake, na Mwenye kujua yanao wafaa.

35 Kisha ikadhihiri rai ya Mheshimiwa na watu wake, baada ya kwisha ona dalili zilizo wazi kuwa Yusuf hana makosa. Wakakubaliana rai hii, na wakaapa kuitimiza. Nayo ni kumtia yeye gerezani kwa muda mfupi au mrefu, ili kumkinga mkewe na maneno mabaya, na kumuepusha na masengenyo ya watu!

36 Wakaingia pamoja na Yusuf vijana wawili katika watumishi wa Mfalme. Mmoja wao akasema: Mimi nimeota usingizini kuwa ninakamua zabibu kutengeneza mvinyo. Mwingine akasema: Mimi nimeota nimebeba kichwani mwangu mikate, na ndege wanaila! Hebu tuambie, ewe Yusuf, tafsiri ya haya tuliyo ota, na mambo yetu yataishia vipi. Sisi tunaamini kuwa wewe ni katika watu wanao sifika kwa wema na kujua tafsiri za ndoto.

37 Yusuf akawaambia kutilia mkazo yale waliyo yajua kwake Yusuf: Hakitowahi kukufikieni chakula kuwa ni riziki mliyo kadiriwa ila nami nitakwambieni kitavyo kujieni kabla ya kukufikieni. Na nitakutajieni mapishi yake na vipi kilivyo. Namna hivyo ndivyo tafsiri ya ndoto na khabari zilizo fichikana katika alivyo nifunza Mola wangu Mlezi na akanifunulia, kwani nilimtakasia Yeye tu ibada yangu. Na nikakataa kumshirikisha na kitu chochote. Na nikajitenga mbali na dini ya watu wasio msadiki Mwenyezi Mungu, na wala hawamuamini Yeye kwa njia iliyo sawa, nao wanaikanya Akhera na hisabu zake.

38 Mimi nimeacha mila ya hawa makafiri, na nikafuata Dini ya baba zangu Ibrahim, na Is-haaq, na Yaa'qub. Nikamuabudu Mwenyezi Mungu pekee. Haitufalii sisi kumfanyia Mwenyezi Mungu mshirika yeyote yule, akiwa Malaika, au jini, au mwanaadamu, licha ya masanamu ambayo hayaleti manufaa wala

39. Enyi wafungwa wenzangu wawili! Je, mabwana wengi wanao farikiana wao kwa wao ni bora au Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye nguvu?³⁹
40. Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyo yapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipo kuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo Dini Iliyo Nyooka. Lakini watu wengi hawajui.⁴⁰
41. Enyi wafungwa wenzangu wawili! Ama mmoja wenu atamnyweshwa bwana wake mvinyo. Na ama mwengine atasulubiwa, na ndege watamla kichwa chake. Imekwisha katwa hukumu ya hilo jambo mlilo kuwa mkiuliza.⁴¹
42. Na akamwambia yule aliye jua kuwa atavuka katika wale wawili: Nikumbuke kwa bwana wako. Lakini Shet'ani alimsahaulisha kumtaja kwa bwana wake. Basi Yusuf akakaa gerezani miaka kadhaa.⁴²
43. Na siku moja mfalme alisema: Hakika mimi nimeota ng'ombe saba wanene wanaliwa na ng'ombe saba walio konda. Na mashuke saba mabichi na mengine makavu. Enyi waheshimiwa! Nambieni maana ya ndoto zangu, ikiwa nyinyi mnaweza kuagua ndoto.⁴³
44. Wakasema: Hizi ni ndoto zilizo paraganyika, wala sisi sio wenye kujua tafsiri ya ndoto hizi.⁴⁴
45. Hapo akasema yule aliye okoka katika wale wawili akakumbuka baada ya muda: Mimi nitakwambieni tafsiri yake. Basi nitumeni.⁴⁵
46. Yusuf! Ewe mkweli! Tueleze nini maana ya ng'ombe saba wanene kuliwa na ng'ombe saba walio konda. Na mashuke saba mabichi na mengine makavu, ili

madhara, wala hayasikii, wala hayaoni! Hiyo ndiyo Tawhidi aliyo tutunukia Mwenyezi Mungu sisi na watu wote, kwa vile alivyo tuamrisha tuwafikilishie ujumbe. Lakini wengi wa watu hawaipokei fadhila hii kwa shukrani, bali wanaikataa!

39 Enyi wenzangu wawili wa gerezani! Je mabwana wengi mbali mbali ni bora mtu kuwanyenyekea kuliko Mwenyezi Mungu Mmoja asiye shindika?

40 Hamuabudu badala ya Mwenyezi Mungu ila majina tu mliyo yazua nyinyi na baba zenu kwa mawazo bila ya kuwepo kweli. Mwenyezi Mungu hakuwateremshia hao hoja wala ushahidi wowote! Hapana wa kuhukumu nini kinacho faa kuabudiwa na kipi hakifai ila Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimnyenyekee yeyote mwenginewe, na mumuabudu Yeye peke yake. Hiyo ndiyo Dini iliyo nzima iliyo nyooka, ambayo dalili zote na ushahidi unaelekea kwake. Lakini aghlabu ya watu hawataki uwongozi wa dalili hizi, wala hawajijui kuwa wamo katika ujinga na upotovu.

41 Enyi wenzangu wawili wa gerezani! Hii basi ndiyo tafsiri ya ndoto zenu: Ama mmoja wenu aliye kamua zabibu katika ndoto yake, atatoka jela, na atakuwa akimnyweshwa mvinyo Mfalme. Na ama huyo wa pili atatundikwa msalabani, na ataachwa msalabani ndege wakimla kichwa chake. Yamekwisha timia hayo mambo kama nilivyo eleza kwa mujibu mliyoy nitaka nieleze tafsiri ya hizo ndoto!

42 Akamwambia yule aliye kuwa atavuka: Nitaje kwa Mfalme kwa sifa zangu, na kisa changu. Asaa huenda akanifanyia insafu akanivua na haya mateso! Shetani alimshughulisha akamsahaulisha kutaja kisa cha Yusuf kwa Mfalme. Basi Yusuf akabaki gerezani kwa miaka isiyo pungua mitatu.

43 Mfalme akasema: Nimeota usingizini kuna ng'ombe saba wanene wanaliwa na wengine saba walio konda madhaifu. Na nimeota mashuke saba mabichi, na mengine saba makavu. Enyi wakuu wanazuoni na wenye maarifa! Nitoleeni fatwa ya hizi ndoto zangu, ikiwa ni kweli nyinyi mnajua tafsiri za ndoto na mnaweza kuzitolea fatwa.

44 Wakasema: Hizi ni ndoto zilizo korogeka ovyo, na wasiwasi wa kuzuka tu katika nafsi ya mtu! Na sisi si wenye kujua tafsiri ya ndoto za ovyo ovyo.

45 Akasema yule mtu aliye okoka katika wawili alio kuwa nao Yusuf gerezani, na akakumbuka wasia wa Yusuf, baada ya kupita muda mrefu: Mimi nitakwambieni tafsiri ya ndoto aliyo itaja mfalme. Nipelekeni kwa huyo mwenye ilimu ya kuifasiri.

nirejeekwa watu wapate kujua.⁴⁶

47. Akasema: Mtalima miaka saba kwa juhudi. Mtacho vuna kiwacheni katika mashuke yake, isipo kuwa kidogo mtacho kula.⁴⁷

48. Kisha itakuja baadaye miaka saba ya shida itakayo kula kile mlichu iwekea isipo kuwa kidogo mtacho kihifadhi.⁴⁸

49. Kisha baada ya haya utakuja mwaka ambao katika mwaka huo watu watasaidiwa, na watakamua.⁴⁹

50. Na mfalme akasema: Mleteni kwangu! Basi mjumbe alipo mjia Yusuf alisema: Rejea kwa bwana wako ukamuulize khabari ya wale wanawake walio jikata mikono yao. Hakika Mola wangu Mlezi anazijua vyema hila zao.⁵⁰

51. Mfalme alisema: Mlikuwa mna nini mlipo mtaka Yusuf kinyume na nafsi yake? Wakasema: *Hasha Lillahi!* Sisi hatukujua ubaya wowote kwake. Mke wa Mheshimiwa akasema: Sasa haki imedhihiri. Mimi ndiye niliye mtaka kinyume na nafsi yake, na hakika yeye ni katika wakweli.⁵¹

52. Hayo ni apate kujua ya kwamba mimi sikumfanyia khiyana nyuma yake; na ya kwamba Mwenyezi Mungu haziongoi hila za makhaini.⁵²

53. NAMI sijitoi lawamani. Kwa hakika nafsi ni mno kuamrisha maovu, isipo kuwa ile ambayo Mola wangu Mlezi aliyu irehemu. Hakika Mola wangu Mlezi ni Msamehevu

46 Yule mtumishi wa kumletea mfalme ulevi akenda kwa Yusuf, akamwita: Yusuf! Ewe uipendaye kweli! Tueleze nini maana ya ndoto ya ng'ombe saba wanene kuliwa na ng'ombe saba walio konda. Na ndoto ya mashuke saba mabichi na mengine makavu? Nataraji kurejea kwa watu nami nina fatwa yako, ili nao wapate kujua maana yake, na waujue ujuzi wako na fadhila yako.

47 Yusuf akasema: Tafsiri ya ndoto hizo ni kuwa mtalima katika ardhi ngano, na shairi kwa muda wa miaka saba mfululizo kwa ukulima wa juhudi. Mtacho vuna kihifadhini, mkiache katika mashuke yake, isipokuwa kidogo mtacho kila katika miaka hiyo, kwa uangalizi mzuri. (*Tazama Maelezo 12:47*)

48 Kisha baada ya miaka hii ya neema itakuja saba ya ukame. Mtakula kile mlichu weka akiba, isipo kuwa kidogo mtacho kificha na kukihifadhi, ili kiwe mbegu ya kupandia baadae.

49 Kisha baada ya miaka hiyo ya ukame utakuja mwaka watu watasaidiwa kwa mvua, na watakamua zabibu na zaituni, na kila cha kukamuliwa.

50 Mfalme akamwona Yusuf atakuwa na faida naye kwa ule uwezo wake kuifasiri ndoto yake, na akaazimia amwite. Akawaamrisha wasaidizi wake wamlete. Alipo mfikia mjumbe akamwambia kuwa mfalme anamtaka, khabari hiyo haikumpapatisha, juu ya kuwa ina bishara ya kufunguliwa kwake. Wala kule kutamani kutoka kwa mfungwa kwenye dhiki za jela na taabu zake hakukuitikisa subira yake. Akakhiari angoje mpaka idhihirike kuwa hana makosa kuliko kufanya haraka kutoka na huku yale aliyo tuhumiwa bado yamemganda. Akamwambia mjumbe: Rejea kwa bwana wako umtake ayaangalie tena yale mashtaka niliyo shitakiwa, awaulize wale wanawake walio kusanywa na mke wa Mheshimiwa kwa kunifanyia hila mimi, wakababaika na wakajikata mikono yao: Je! Walipo toka kwenye yale majaribio walikuwa wanaamini kuwa mimi sina makosa na safi, au waliniona ni mchafu na mzinifu? Mimi nataka haya ipate kuonekana hakika katika macho ya watu. Ama Mola wangu Mlezi anavijua vyema vitimbi vyao!

51 Mfalme akawakusanya wale wanawake, na akawauliza: Ilikuwa vipi hali yenu pale mlipo jaribu kumhadaa Yusuf aghafilike na wema wake na usafi wa nafsi yake? Je, mlimwona amemili kwenu? Wakamjibu: Mwenyezi Mungu ametakasika! Hakumsahau mja wake hata uchafuke usafi wake. Sisi hatukuona kwake lolote la kumtia dosari. Hapo basi wema ukapata nguvu katika moyo wa Zuleikha (mke wa Mheshimiwa) akaingia kusema: Sasa kweli imedhihiri! Ni mimi ndiye niliye mkhadaa, na nikajaribu kumzaini kinyume na nafsi yake kwa kumghuri. Lakini yeye alishikilia usafi wake! Na sasa nahakikisha kuwa yeye ni katika watu wa kweli. Na ni haki tupu alipo nirudishia tuhuma mimi na kunitia makosani!

52 Haya mimi naungama kwa kweli ninayo itoa, apate kuwa na yakini Yusuf kuwa mimi sikuchukua fursa ya kuto kuwepo alipo kuwa gerezani nikaendelea na khiyana, na nikamdhulumu kwa kumtuhumu. Na kwa kuwa hakika Mwenyezi Mungu haijaalii kufanikiwa mipango ya makhaini.

na Mwenye kurehemu.⁵³

54. Basi mfalme akasema: Mleteni kwangu, awe wangu mwenyewe khasa. Basi alipo msemiza alinena: Hakika wewe leo umekwisha tamakani kwetu na umeaminika.⁵⁴

55. Yusuf akasema: Nifanye mshika khazina za nchi. Kwani hakika mimi ni mlinzi mjuzi.⁵⁵

56. Basi namna hivi tukampa Yusuf cheo katika nchi; anakaa humo popote anapo penda. Tunamfikishia rehema zetu tumtakaye, wala hatupuuzi malipo ya wafanyao mema.⁵⁶

57. Na hakika malipo ya Akhera ni bora zaidi, kwa walio amini na wakawa wachamngu.⁵⁷

58. Wakaja ndugu zake Yusuf, na wakaingia kwake. Yeye akawajua na wao hawakumjua.⁵⁸

59. Na alipo watengeneza tayari haja yao alisema: Nileteeni ndugu yenu kwa baba. Je! Hamwoni ya kwamba mimi ninatimiza kipimo, nami ni mbora wa kukirimu?⁵⁹

60. Na msipo niletea basi hampati kipimo chochote kwangu, wala msinikurubie.⁶⁰

61. Wakasema: Sisi tutamirai baba yake; na bila ya shaka tutafanya hayo.⁶¹

62. Na Yusuf akawaambia watumishi wake: Tieni bidhaa zao katika mizigo yao, ili

53 Wala sidai kuwa nafsi yangu haitelezi; kwani ni tabia ya nafsi kumili kwenye matamano, na kupendelea maovu na shari. Isipo kuwa nafsi aliyo ilinda Mwenyezi Mungu na akaiweka mbali na maovu. Na hakika mimi ninatumai rehema ya Mwenyezi Mungu na msamaha wake, kwani Yeye ni Mkunjufu wa kusamehe dhambi za wenye kutubu, na yu karibu wa kuwarehemu waja wake walio kosa.

54 Usafi wa Yusuf ulipo dhiri kwa mfalme, aliazimu amwite. Akawatuma watu wake wamlete awe wake yeye mwenyewe wa kumsafia niya. Basi alipo hudhuria na yakapita baina yao mazungumzo, mfalme akaathirika na utukufu wa Yusuf kwa usafi wa nafsi yake, na ubora wa rai zake! Akamwambia: Sasa wewe kwangu utakuwa na cheo cha hishima kilicho thibiti. Na wewe ni muaminifu kwangu ninaye kuamini.

55 Mfalme akajua kwake Yusuf kuwa yeye ni muangalizi mwema na mweza wa kazi yake. Na Yusuf akahisi hayo. Hapo akataka amfanye waziri akamwambia: Nitawalishe juu ya khazina zote za mamlaka yako, na ghala za nchi yako. Kwani mimi kama ulivyo yakinika mwenyewe naweza kuendesha mambo ya serikali, nami ni mlinzi, na najua kupanga na kuendesha mambo.

56 Mfalme alilikubali ombi lake, akamfanya waziri wake. Hivyo basi Mwenyezi Mungu alimneemesha Yusuf kwa neema nzuri, akampa madaraka na uwezo katika nchi ya Misri, akienda humo atakapo. Na hii ndiyo shani yake Mwenyezi Mungu kwa waja wake, humpa neema yake amtakaye katika wao, wala hawanyimi thawabu zao, bali huwapa ujira wao wa wema wautendao kwa kuwalipa mema hapa hapa duniani.

57 Na malipo yao ya Akhera ni bora zaidi na yanalingana zaidi na hao wanao msadiki Yeye na Mitume wake, na ikawa wanaingojea Siku ya Hisabu na wanaikhofu.

58 Ukame ukazidi kushtadi katika nchi jirani na Misri. Ikawapata watu wa Yaa'qub shida vile vile kama ilivyo wapata wengineo. Watu walikwenda Misri kutoka kila pande baada ya kujua matengenezo ya Yusuf ya kuweka akiba chakula, na kujitayarisha kwake kwa miaka ya ukame. Yaa'qub aliwatuma wanawe wende kutafuta chakula, lakini akabaki naye nduguye Yusuf kwa mama kwa kumkhofia. Wale watoto wake walipo fika Misri wakenda moja kwa moja kwa Yusuf, naye akawatambua, lakini wao hawakumjua.

59 Yusuf akaamrisha wakaribishwe ugeni, na wapewe mahitaji wanayo yataka. Wakapewa hayo. Akaingia kuzungumza nao na kuwauliza hali zao kama mtu asiye wajua! Naye anawajua vyema. Nao wakamwambia kuwa wamemwacha ndugu yao mmoja kwa baba yao, kwani hapendi kuachana naye. Naye huyo ni Bin-yamini nduguye Yusuf kwa baba na mama. Basi yeye akasema: Mwacheni ndugu yenu aje nanyi, wala msigope chochote. Nyinyi mmekwisha ona vipi ninavyo kutimizieni vipimo vyenu, na ninavyo kukirimuni.

60 Mkitomleta ndugu yenu huyu, basi hampati chakula kwangu, wala msijaribu kunijia tena.

61 Nduguze wakasema: Tutajaribu kusema na baba yake ageuze rai yake, iondoke khofu yake juu ya mwanawe. Na sisi tunakuhakikishia kuwa hatutokasiri wala kulegalega katika hayo.

wazione watakapo rudi kwa watu wao wapate kurejea tena.⁶²

63. Basi walipo rejea kwa baba yao, walisema: Ewe baba yetu! Tumenyimwa chakula zaidi, basi mpeleke nasi ndugu yetu ili tupate kupimiwa; na yakini sisi tutamlinda.⁶³

64. Je, nikuaminini kwa huyu ila kama nilivyo kuaminini kwa nduguye zamani? Lakini Mwenyezi Mungu ndiye Mbora wa kulinda, naye ndiye Mbora wa kurehemu kuliko wenye kurehemu wote.⁶⁴

65. Na walipo fungua mizigo yao wakakuta bidhaa zao wamerudishiwa. Wakasema: Ewe baba yetu! Tutake nini zaidi? Hizi bidhaa zetu tumerudishiwa. Wacha tuwalettee watu wetu chakula, na tutamlinda ndugu yetu, na tutaongeza shehena ya ngamia. Na hicho ni kipimo kidogo.⁶⁵

66. Akasema: Sitampeleka nanyi mpaka mnipe ahadi kwa Mwenyezi Mungu kwamba lazima mtamrejea kwangu, ila ikiwa mmezungukwa. Basi walipo mpa ahadi yao alisema: Mwenyezi Mungu ndiye Mtegemewa kwa tuyasemayo.⁶⁶

67. Na akasema: Enyi wanangu! Msiingie mlango mmoja, bali ingieni kwa milango mbali mbali. Wala mimi sikufaeni kitu mbele ya Mwenyezi Mungu. Hukumu haiko ila kwa Mwenyezi Mungu tu. Juu yake Yeye mimi nimetegemea, na juu yake Yeye wategemea wanao tegemea.⁶⁷

62 Walipo taka kuondoka aliwaambia wafwasi wake: Watilieni thamani ya bidhaa yao waliyo kuja nayo humo humo pamoja na mizigo yao, ili waione watakapo rudi kwa watu wao, wapate kurejea tena kwa kutumai kupewa chakula kwa kuamini kuwa tunatimiza ahadi, na wawe na imani ya usalama wa ndugu yao, na baba yao azidi kutua nafsi yake.

63 Walipo rejea kwa baba yao walimsimulia kisa chao na Mheshimiwa wa Misri, na upole wake kwao, na kwamba amewaonya kuwa atawanyima kuwapimia chakula baadae ikiwa hatokuwa nao Bin-yamini; na kwamba amewaahidi kuwatimizia kipimo na atawatukuza pindi wakirudi na ndugu yao. Wakamwambia baba yao: Mwache ende nasi ndugu yetu, kwani ukimpeleka yeye tutapimiwa chakula cha kutosha tunacho kihitajia. Nasi tunakuahidi ahadi ya nguvu ya kwamba tutafanya juhudi kumlinda.

64 Yaa'qub yalimtibuka moyoni mwake yale ya zamani, akayaunganisha na haya mapya. Akawaambia wanawe: Nikikukubalieni itakuwa hali yangu ni ya ajabu; kwani nikikuaminini kwa huyu ndugu yenu haitakuwa ila mfano wa pale nilipo kuaminini kwa Yusuf. Mkamchukua kisha mkarudi mkisema: Kaliwa na mbwa mwitu! Lakini Mwenyezi Mungu ndiye anaye nitosheleza katika kumlinda mwanangu. Wala mimi simtegemei mtu ila Yeye, kwani Yeye ndiye Mlinzi aliye na nguvu kuliko wote, na rehema yake ni kunjufu mno, hatonipa tena machungu ya ndugu yake baada ya yale ya Yusuf.

65 Na wale nduguze Yusuf hawakujua kuwa Yusuf aliwatilia bidhaa zao katika mizigo yao. Walipo ifungua wakakuta mali yao, na wakaona hisani aliyo wafanyia Yusuf, wakaitemia hiyo kuzidi kumpoza moyo Yaa'qub, na kumkinaisha awakubalie kwa aliyo yataka Mheshimiwa. Wakazidi kumshikilia akubali, wakamkumbusha makhusiano yao yalio wafunga kwa baba mmoja. Wakasema: Ewe baba yetu! Unataka wema gani zaidi kuliko haya, na hayo yatayo kuwa? Haya mali yetu tumerudishiwa bila ya kuchukuliwa chochote. Basi natusafiri na ndugu yetu, na tuwalettee watu wetu mahitaji, nasi tutamchungu ndugu yetu, na tutaongeza mahitaji shehena ya ngamia kuwa ni haki ya ndugu yetu! Kwani yule Mheshimiwa kapanga kuwa kila mtu humpa shehena ya ngamia.

66 Waliweza wana wa Yaa'qub kumkinaisha baba yao, na maneno yao yakampata palipo. Akaacha kushikilia kumzuia mwanawe asende Misri na nduguze. Lakini moyo wake haukuwacha kuwa na haja ya kuzidi kutuzwa. Kwa hivyo aliwaambia: Sitomwacha ende nanyi ila baada ya kunipa dhamana ya nguvu. Niahidini kwa Mwenyezi Mungu kwamba mtanirudishia mtapo rudi. Na wala msiache kumrudisha ila mkiangamia nyinyi au ikawa adui amekuzungukeni akakushindeni. Wakamkubalia na wakampa ahadi aliyo itaka. Na hapo tena akamshuhudisha Mwenyezi Mungu ahadi yao na viapo vyao kwa kusema: Mwenyezi Mungu anayashuhudia na kuyaona yote haya yanayo pita baina yetu.

67 Yaa'qub alitua kwa ahadi ya watoto wake. Kisha huruma ilimpelekea kuwausia kuwa watapo ingia Misri waingie kupita milango mbali mbali, ili watu wasiwapige kijicho, huenda wakadhurika. Akasema: Wala mimi sina uwezo wa kukulindeni na madhara. Kwani mwenye kuzuia madhara ni Mwenyezi

68. Na walipo ingia kama alivyo waamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu, isipo kuwa ni haja tu iliyo kuwa katika nafsi ya Yaa'qub aliitimiza. Na hakika yeye alikuwa na ilimu kwa sababu tulimfundisha; lakini watu wengi hawajui.⁶⁸

69. Na walipo ingia kwa Yusuf alimchukua nduguye akasema: Mimi hakika ni nduguyo. Basi usihuzunike kwa waliyo kuwa wakiyafanya.⁶⁹

70. Na alipo kwisha watengenezea mahitaji yao akakitia kikopo cha kunywea maji katika mzigo wa nduguye huyo, kisha mnadi akanadi: Enyi wasafiri! Hapana shaka nyinyi ni wezi!⁷⁰

71. Wakasema nao wamewakabili: Kwani mmepoteza nini?⁷¹

72. Wakasema: Tumepoteza kopo la mfalme. Na ataye lileta atapewa shehena nzima ya ngamia. Nami ni dhaamini wa hayo.⁷²

73. Wakasema: Wallahi! Mnajua vyema kwamba sisi hatukuja kufanya uharibifu katika nchi hii, wala sisi si wezi.⁷³

74. Wakasema: Basi malipo yake yatakuwa nini ikiwa nyinyi ni waongo?⁷⁴

75. Wakasema: Malipo yake ni yule ambaye ataonekana nalo yeye huyo ndiye malipo yake. Hivi ndivyo tunavyo walipa madhaalimu.⁷⁵

76. Basi akaanza kwenye mizigo yao kabla ya mzigo wa nduguye. Kisha akakitoa katika mzigo wa nduguye. Hivi ndivyo tulivyo mpangia Yusuf. Hakuweza kumzuia nduguye

Mungu tu, na hukumu ni yake Yeye pekee. Mimi nimeategemea Yeye, na mambo yangu na yenu yote nime mwachia Yeye. Na juu yake Yeye peke yake wategemea wote wanao tegemeza mambo yao, kwa kumuamini Yeye.

68 Wale vijana wakapokea wasia wa baba yao, wakapitia milango mbali mbali. Wala hayo si kama ndiyo ya kuwazuilia madhara walio kwisha andikiwa na Mwenyezi Mungu! Na Yaa'qub akijua hayo, kwani yeye alikuwa na ilimu tuliyo mfundisha. Lakini wasia wake ulikuwa ni kwa haja aliyokuwa nayo nafsiini mwake tu, nayo ni huruma ya baba kwa wanawe ambayo ameidhihirisha katika huu wasia. Na hakika watu wengi hawana ujuzi kama alio kuwa nao Yaa'qub wakamwachia mambo yao Mwenyezi Mungu awalinde.

69 Walipo ingia kwa Yusuf aliwapokea kwa hishima, na khasa yule nduguye kwa baba na mama ndio akamchukua na akampa siri kwa kumwambia: Usitie shaka mimi ni nduguyo Yusuf. Basi usihuzunike kwa waliyo kufanyia wewe na waliyo nifanyia mimi.

70 Basi baada ya kuwakirimu kwa kuja kwao, na kuwapimia chakula, na kuwazidishia shehena ya nduguye, aliwafungia mizigo yao kwa ajili ya safari. Tena akawaamrisha wasaidizi wake watumbukize chombo cha kunywea katika mzigo wa Bin-yamini. Kisha mmoja wa wasaidizi wa Yusuf alinadi: Enyi wasafiri! Ngojeni! Nyinyi ni wezi.

71 Wakashituka nduguze Yusuf kwa kutangaziwa yale, wakawaelekea wale wenye kunadi wakawauliza: Mmepoteza nini, na mnatafuta nini?

72 Wale wasaidizi wakajibu: Tunatafuta kikopo, nacho ni chombo anacho nywea mwenyewe mfalme. Na malipo yake kwa mwenye kukileta ni shehena nzima ya chakula anayo ibeba ngamia. Yule mkubwa wao alitilia mkazo hayo kwa kusema: Na mimi ninadhamini kutimiza ahadi hii.

73 Nduguze Yusuf wakasema: Hakika kututuhumu sisi kwa wizi ni jambo la ajabu mno! Na tunahakikisha kwa kiapo ya kwamba nyinyi wenyewe mmeona katika mwendo wetu na tunavyo ishika dini yetu katika mara mbili tulipo kuja hapa kuwa mmejua yakini kuwa sisi hatutaki kuleta uharibifu katika nchi yenu. Wala si katika tabia yetu kuwa ni wezi.

74 Na Yusuf alikwisha waamrisha wafwasi wake wawaache nduguze waamue nini malipo anayo stahiki kupata yule atakaye onekana nacho kile kikopo, ili apate kumchukua nduguye kwa hukumu yao wenyewe, na iwe hukumu yao ndiyo ya kukata shauri, isiwepo njia ya kumwomba. Basi watu wa Yusuf wakawaambia wale nduguze: Nini malipo ya wevi kwenu wanapo gundulikana ni katika nyinyi?

75 Na kwa kuwa wana wa Yaa'qub walikuwa na yakini kuwa wao hawakukiba kile kikopo walisema bila ya kusitasita: Malipo ya mwenye kuchukua hicho kikopo ni kushikwa huyo na afanywe mtumwa. Ndio hivi sisi tunavyo walipa wenye kudhulumu wakachukua mali ya watu.

kwa sharia ya mfalme isipo kuwa alivyo taka Mwenyezi Mungu. Tunawatukuza kwenye vyeo tuwatako; na juu ya kila ajuaye yupo ajuaye zaidi.⁷⁶

77. Wakasema: Ikiwa huyu ameiba, basi nduguye vile vile aliiba zamani. Lakini Yusuf aliyaweka siri moyoni mwake wala hakuwaonyesha. Akawaambia: Nyinyi mko katika hali mbaya zaidi, na Mwenyezi Mungu anajua zaidi hayo mnayo singizia.⁷⁷

78. Wakasema: Ewe Mheshimiwa! Huyu anaye baba mzee sana. Kwa hivyo mchukue mmoja wetu badala yake. Hakika sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.⁷⁸

79. Akasema: Mwenyezi Mungu apishe mbali kumshika yeyote yule isipo kuwa tuliye mkuta naye kitu chetu. Hivyo basi tutakuwa wenye kudhulumu.⁷⁹

80. Walipo kata tamaa naye wakenda kando kunong'ona. Mkubwa wao akasema: Je! Hamjui ya kwamba baba yenu amechukua ahadi kwenu kutokana na Mwenyezi Mungu, na kabla ya hapo mlimkosa katika agano lenu juu ya Yusuf? Basi mimi sitotoka nchi hii mpaka baba yangu anipe ruhusa au Mwenyezi Mungu anihukumie. Na Yeye ndiye Mbora wa mahakimu.⁸⁰

81. Rudini kwa baba yenu, na mwambieni: Ee baba yetu! Mwanao ameiba. Na sisi hatutoi ushahidi ila kwa tunayo yajua. Wala sisi hatukuwa wenye kuhifadhi mambo

76 Shauri ikaishia ipekuliwe mizigo, na ikawa lazima kufanya mambo baraabara ili isionekane kuwa kuna mpango ulio pangwa. Yusuf mwenyewe ndiye aliye fanya uchunguzi, baada ya kwisha tengeza mambo. Akaanza kupekua mizigo ya wale ndugu kumi, kisha ndio akaingia kuupekua mizigo wa nduguye. Humo akakitoe kile kikopo, na kwa hivyo hila yake ikafuzu. Akawa na haki kwa hukumu ya nduguze kumshika Bin-yamini. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu alivyo mpangia mambo Yusuf. Hakuwa anaweza yeye kumshika nduguye kwa mujibu wa sharia ya mfalme wa Misri tu ila kwa kutaka Mwenyezi Mungu. Naye alitaka. Basi tulimpangia mambo Yusuf, na tukamwezesha kuzirekibisha sababu na mipango baraabara na hila nzuri. Na haya ni katika fadhila za Mwenyezi Mungu, ambaye humtukuza katika vyeo vya ujuzi amtakaye. Na juu ya kila mwenye ilimu yupo mwenye kumzidia katika ujuzi!

77 Kule kugunduliwa kikopo katika mzigo wa ndugu yake kwa ghafla kuliwashangaza nduguze na kukawababisha. Kwa hivyo wakataka kujivua kuwa wao wote hawana makosa ila huyo na Yusuf, na kusema kuwa tabia ya wizi wameirithi kwa mama yao. Wakasema: Si ajabu kuwa huyo kaiba, kwani nduguye khalisa aliwahi kwiba vile vile! Na Yusuf akatambua kijembe chao wanacho mpigia, na yakamuudhi hayo. Lakini aliyaficha, na akawawekea jawabu moyoni mwake lau kuwa amesema wazi jawabu yenyewe inge kuwa hivi: Nyinyi mko katika hali ova zaidi, na nyinyi ni duni zaidi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua vyema, na kutambua ukweli wa maneno yenu ya kumsingizia nduguye fedheha ya wizi.

78 Wakawa hawana budi kujaribu kumvua ndugu yao au kumtolea fidia kwa kutaka kutimiza ile ahadi yao waliyo mpa Yaa'qub. Wakaingia kutaka kumlainisha moyo Yusuf kwa kumtaja uzee wa baba yao, wakamwambia: Ewe Mheshimiwa! Huyu ndugu yetu ana baba mtu mzima sana. Basi mfanyie huruma umchukue mmoja wetu mwengineawe awe badala ya mwanawe huyu ambaye ndiye anaye mpenda moyoni mwake. Matarajio yetu ni kuwa utatukubalia mambo yetu. Kwenu tumekwisha ona tabia yako ya ukarimu, na tumehakikisha mwendo wako wa kupenda kufanya hisani na kutenda mema.

79 Wala haikufalia kwa Yusuf kuvunja mpango alio mkubalia Mwenyezi Mungu, na kumwachia nduguye atoke mkononi mwake. Kwa hivyo maombi yao hayakumlainisha kitu. Akawajibu jawabu mkato, kwa kuwaambia: Mimi najilinda kwa Mwenyezi Mungu isije nafsi yangu ikadhulumu kwa kumzuia yeyote yule isipo kuwa yule yule tuliye mkuta nayo mali yetu. Tukimchukua mwenginewe kwa kumuadhibu tutakuwa katika hao walio vuka mipaka kwa kumshika asiye na makosa kwa madhambi ya mwovu.

80 Iliipo katika tamaa yao, wakavunjika moyo kukubaliwa maombi yao, wakenda pembeni peke yao wakishauriana juu ya msimamo wao na baba yao. Iliipo ishia shauri kwa mkubwa wao mwenye kupanga mambo yao, aliwaambia: Haikufalieni kuisahau ahadi ya kiapo mliyo mpa baba yenu ya kuwa mtamhifadhi ndugu yenu mpaka mrudi naye, wala mlivyo fungana naye kabla yake kuwa mtamlinda Yusuf, na hayo mkayavunja! Kwa hivyo mimi nitabaki Misri wala sitotoka ila afahamu baba yetu ukweli wa hali hii, na akaniachilia nirejee kwake, au Mwenyezi Mungu anihukumie kurejea kwa hishima, na akanisahilishia njia kwa sababu yoyote ile. Na Yeye ndiye Mbora wa uadilifu kuliko mahakimu wote.

ya ghaibu.⁸¹

82. Na waulize watu wa mji tulio kuwako, na msafara tulio kuja nao. Na hakika sisi tunasema kweli.⁸²

83. Akasema: Bali nafsi zenu zimekushawishini kwenye jambo fulani. Subira ni njema! Asaa Mwenyezi Mungu akaniletea wote pamoja. Hakika Yeye ni Mjuzi Mwenye hikima.⁸³

84. Naye akajitenga nao, na akasema: Ah! Masikini Yusuf! Na macho yake yakawa meupe kwa huzuni aliyo kuwa akiizuia.⁸⁴

85. Wakasema: Wallahi! Huachi kumkumbuka Yusuf mpaka uwe mgonjwa au uwe katika walio hiliki.⁸⁵

86. Akasema: Hakika mimi namshitakia Mwenyezi Mungu sikitiko langu na huzuni yangu. Na ninajua kwa Mwenyezi Mungu msiyo yajua nyinyi.⁸⁶

87. Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye, wala msikate tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu. Hakika hawakati tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu isipo kuwa watu makafiri.⁸⁷

88. Basi walipo ingia kwa Yusuf walisema: Ewe Mheshimiwa! Imetupata shida, sisi

81 Rejeeni nyinyi kwa baba yenu, na msimulieni kisa chote hichi. Na mwambieni: Mkono wa mwanao ulikunjuka akakiiba kikopo cha mfalme, na kimekutikana katika bahasha yake. Kwa huo wizi wake ndio ameshikwa. Nasi hatukwambii ila tuliyo yaona, na wala sisi hatukuwa tunajua yaliyo fichikana katika hukumu ya Mwenyezi Mungu pale tulipo kutaka nawe ukatupa tumhifadhi na turejee naye kwako kama tulivyo ahidiana na tukafungana. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mbora wa uadilifu kuliko mahakimu wote.

82 Na ikiwa wewe una shaka na haya tunayo kwambia mtume mtu akuletee ushahidi wa watu wa Misri. Na pia wewe mwenyewe waulize wasafiri wenzetu tulio rudi nao, ipate kudhiri kuwa sisi hatuna lawama. Nasi tunakuhakikishia kuwa sisi ni wakweli katika haya tuyasemayo.

83 Wakarejea wana walio baki kwa Yaa'qub. Wakamueleza kama alivyo wausia kaka yao mkubwa. Khabari ile ikamtibua huzuni zake, zikazidi kwa kumpoteza mwanawe wa pili. Wala hakutua nafsi yake kwa kuwa wao hawana makosa ya kusabibisha kupotea kwake, naye angali na machungu kwa waliyo mfanyia Yusuf. Akapiga ukelele kwa kuwatuhumu akiwaambia: Niya yenu haikusalimika katika kumhifadhi mwanangu, lakini nafsi zenu zimekuchocheeni mumpoteze kama mlivyo mpoteza nduguye. Lau kuwa nyinyi hamkutoa fatwa ya kuwa mwizi ashikwe afanywe mtumwa kuwa ndiyo adabu ya mwizi huyo Mheshimiwa asingeli mshika mwanangu, wala asingeli baki kaka yenu huko Misri. Lakini mimi sina hila ila kustahamili katika msiba wangu kwa maliwaza mema, huku nikitaraji kwa Mwenyezi Mungu anirudishie wanangu wote. Kwani Yeye ndiye Mwenye ujuzi ulio zunguka hali yangu na hali zao. Na Yeye ndiye Mwenye hikima yenye kushinda, na kwa hiyo ndio hunitendea na hunipangia.

84 Akadhikika kwa waliyo yasema, akajitenga nao, kashughulika na msiba wake na huzuni kumkosa Yusuf. Macho yake yakafanya kiza kwa wingi wa huzuni, naye akiificha sana. (*Tazama Maelezo 12:84*)

85 Siku zikapita na Yaa'qub kazama katika majonzi yake. Wanawe wakaogopa isije kuwa khatari. Wakamkabili kumtaka apunguze huzuni yake, nao wako baina ya kumwonea huruma na kuchukua kuwa bado yu ngali akimkumbuka Yusuf wakamwambia: Kama hukujipunguzia nafsi yako hapana shaka kumkumbuka Yusuf kutakuzidishia machungu yako yakukondeshe mpaka ukaribie kufa, au ufe khasa!

86 Maneno yao hayakumuathiri hata chembe. Akawajibu kwa kusema: Mimi sikukushitakieni, wala sikukutakeni mnipunguzie machungu yangu! Mimi sina ila Mwenyezi Mungu tu wa kumnyenyekea na kumshitakia dhiki zangu nzito na nyepesi. Wala siwezi kumficha hayo wala lolote nisilo liweza, kwani mimi natambua wema wake wa kutenda na ukunjufu wa rehema yake, jambo ambalo nyinyi hamlijui!

87 Na kuwa na imani na Mwenyezi Mungu ndio huhuisha matumaini. Kwa hivyo zile dhiki za moyo hazikuondoka kwa matarajio ya Yaa'qub kumrudia wanawe, na yakamtia katika moyo wake kuwa wangali wawai, na kwamba wakati wa kukutana nao ndio umefika. Akawaamrisha wanawe wende wakawatafute, akawaambia: Enyi wanangu! Rejeeni Misri muwe na kaka yenu, na mumtafute Yusuf na nduguye, muulize khabari zao kwa upole bila ya watu kujua. Wala msikate tamaa kwa Mwenyezi Mungu kuturehemu kwa kuwarudisha. Kwani hawakati tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu isipo kuwa wale wanao kanya.

na watu wetu. Na tumeleta mali kidogo. Basi tupimie kipimo na fanya kama unatupa sadaka. Hakika Mwenyezi Mungu huwalipa watoao sadaka.⁸⁸

89. Akasema: Je! Mmejua mliyo mfanyia Yusuf na nduguye mlipo kuwa wajinga?⁸⁹

90. Wakasema: Kumbe wewe ndiye Yusuf? Akasema: Mimi ndiye Yusuf, na huyu ni ndugu yangu. Mwenyezi Mungu ametufanyia hisani. Hakika anaye mcha Mungu na akasubiri, basi Mwenyezi Mungu haachi ukapotea ujira wa wafanyao mema.⁹⁰

91. Wakasema: Wallahi! Mwenyezi Mungu amekufadhilisha wewe kuliko sisi, na hakika sisi tulikuwa wenye kukosa.⁹¹

92. Akasema: Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu.⁹²

93. Nendeni na kanzu yangu hii na mumwekee usoni baba yangu, atakuwa mwenye kuona. Na mje nao watu wenu wote wa nyumbani.⁹³

94. Na ulipo ondoka tu msafara baba yao alisema: Hakika mimi nasikia harufu ya Yusuf, lau kuwa hamtanituhumu.⁹⁴

95. Wakasema: Wallahi! Hakika bado ungali katika upotovu wako wa zamani.⁹⁵

88 Nduguze Yusuf walimwitikia baba yao kwa matakwa yake. Wakatoka kwenda Misri, na wakajaribu kukutana na mtawala wake ambaye baadae ikadhihiri kuwa ndiye Yusuf! Walipo ingia kwake walisema: Ewe Mheshimiwa! Sisi na watu wetu tumepata shida ya njaa na madhara ya mwili na nafsi. Na tumekuletea mali chache ndio bidhaa yetu. Nayo ni ya kukataliwa kwa kuwa ni kidogo na mbaya, wala haitoshi kwa hayo tunayo taraji kwako. Lakini sisi tunataraji kwako utupimie kwa ukamilifu na utacho tuzidishia kiwe ni sadaka unayo tupa. Kwani hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu huwalipa wenye kutoa sadaka thawabu njema kabisa.

89 Yusuf akaingiwa na huruma ya udugu ambayo inasamehe maovu. Akaanza kuwafunulia khabari zake kwa kuwaambia kwa lawama: Je! Mmejua ule uovu mliyo mfanyia Yusuf kwa kumtumbukiza kisimani, na maudhi mlio mfanyia nduguye, mkafanya hayo kwa ujinga ulio kusahaulisheni huruma na udugu?

90 Kuzinduliwa huku kwa furaha kuliwatambulisha kwamba huyu ndiye Yusuf. Wakamtazama kisha wakasema kwa yakini: Hakika wewe ndiye kweli Yusuf! Na Yusuf mwenye ukarimu aliwaambia kwa kuwakubalia: Mimi ndiye Yusuf, na huyu ni ndugu yangu. Mwenyezi Mungu ametufadhili kwa kutuvua kwa salama tushilikiki, na kwa kutupa hadhi na madaraka! Na hayo yamekuwa ni malipo ya Mwenyezi Mungu kwa usafi wangu na wema wangu. Na hakika Mwenyezi Mungu haachi ukapotea ujira wa mtendaji mema na akaendelea nao.

91 Wakasema: Uliyo sema ni kweli, na tunakuhakikishia kwa kiapo kwamba hapana shaka Mwenyezi Mungu amekutukiza kwa uchamngu, na subira, na sera njema. Na amekupa pia utawala na cheo cha juu. Na sisi hakika tulikuwa wenye kutenda dhambi kwa tuliyo kutendea wewe na nduguyo. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu ametudhalilisha kwako, na ametulipa malipo ya wenye kutenda dhambi.

92 Yule Nabii mtukufu akawajibu kwa kusema: Hapana lawama kwenu leo, wala kusutana. Lenu kutoka kwangu ni msamaha ulio mwema kwa fadhila ya nasaba na haki ya udugu. Na namuomba Mwenyezi Mungu akusameheni na akughufirieni. Na Yeye ndiye Mwenye rehema kuu.

93 Kisha Yusuf akawaauliza khabari za baba yao. Walipo mwambia kuwa hali yake ni mbaya na hawezi kuona kwa wingi wa hamu na majonzi, aliwapa kanzu yake, na akawaambia: Rejeeni kwa baba yangu, na hii kanzu mwekeeni usoni pake. Kwa hivyo atakuwa na yakini kuwa mimi nimo katika salama, na moyo wake utajaa furaha, na Mwenyezi Mungu atamjaalia iwe ni sababa ya kurejea kuona kwake. Hapo tena njooni naye kwangu, na ahali zenu wote pamoja.

94 Wakaondoka na ile kanzu. Na moyo wa Yaa'qub ulikuwa umezama kungojea nini litalo leta safari ya wanawe. Na Mwenyezi Mungu alikuwa yu pamoja naye katika kungojea huko, ikawa roho yake imeshikamana na roho zao. Basi ule msafara wao ulipo toka nchi ya Misri katika njia yake kumwendea yeye, aliwaambia ahali zake hayo kwa kusema: Mimi naihisi harufu ninayo ipenda ya Yusuf inanijaa. Na lau kuwa sikhofu kwamba mtanituhumu kwa niyasemayo ningeli kwambieni mengi ya Yusuf kuliko hizi hisiya na mawazo.

95 Wale ahali zake wakamjibu jawabu kali wakiapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa yeye yu ngali kuropokwa kwake na kupiswa kwake kwa uzee! Basi akajitayarisha alivyo jitayarisha kwa mapenzi yake yaliyo pita

96. Basi alipo fika mbashiri na akaiweka kanzu usoni pake alirejea kuona. Akasema: Je! Sikukwambieni kuwa mimi najua ya Mwenyezi Mungu msiyo yajua nyinyi?⁹⁶

97. Wakasema: Ee baba yetu! Tuombe msamaha kwa dhambi zetu. Hapana shaka sisi tulikuwa na makosa.⁹⁷

98. Akasema: Nitakuja kuombeeni msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ndiye Mwenye maghfira na Mwenye kusamehe.⁹⁸

99. Na walipo ingia kwa Yusuf aliwakumbatia wazazi wake na akasema: Ingieni Misri, Inshallah, mmo katika amani.⁹⁹

100. Na akawapandisha wazazi wake kwenye kiti cha enzi. Na wote wakaporomoka kumsujudia. Na akasema: Ewe baba yangu! Hii ndiyo tafsiri ya ile ndoto yangu ya zamani. Na Mwenyezi Mungu ameijaalia iwe kweli. Na Mwenyezi Mungu amenifanyia wema kunitoa gerezani, na kukuleteni kutoka jangwani baada ya Shet'ani kuchocha baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mpole kwa alitakalo. Bila ya shaka Yeye ni Mjuzi Mwenye hikima.¹⁰⁰

101. Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika umenipa utawala, na umenifunza tafsiri ya mambo. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema.¹⁰¹

kiasi ya kumpenda Yusuf, na kuendelea kwake kumkumbuka na kutaraji kukutana naye.

96 Akashikilia tamaa yake akingojea rehema ya Mwenyezi Mungu, na ahali zake wakashikilia kumdhania dhana mbovu mpaka alipo fika mtu aliye chukua kanzu na kumbashiria kwamba Yusuf yupo salama salmina. Ilipo wekwa kanzu usoni kwa Yaa'qub akainusa harufu yake, moyo wake ulijaa furaha, macho yake yakarejea kuona. Yule mjumbe alipo msimulia hali ya Yusuf, na kwamba anamtaka yeye asafiri ende pamoja na ahali zake, aliwageukia walio kuwa naye akiwakumbusha ule utabiri wake, na akiwakaripia kwa vile walivyo mkadhibisha. Akawataka wakumbuke yale aliyi wahakikishia pale punde kwamba yeye anajua rehema ya Mwenyezi Mungu na fadhila yake wasio ijua wao.

97 Hapo wakambabili kwa kumtaka msamaha, wakimtaraji awasamehe, na awatakie kwa Mwenyezi Mungu maghfira kwa madhambi yao. Kwani wao walimhakikishia katika kule kutubu kwao kwamba wao walikuwa ni wenye kutenda madhambi.

98 Akasema Yaa'qub nitaendelea kutaka msamaha kwa Mwenyezi Mungu kufutiwa dhambi zenu. Na hakika Yeye peke yake ndiye mwenye maghfira ya milele na rehema ya daima.

99 Yaa'qub akasafiri kwenda Misri pamoja na ahali zake mpaka akafika huko. Walipo ingia kwa Yusuf, naye alikuwa kawapokea kwenye milango ya Misri, huruma na shauku ilimpeleka kwa haraka kwa baba na mama yake! Akawakaribisha na akawataka wao na ahali zake wakae Misri kwa amani na salama kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

100 Msafara ukenda ndani ya nchi ya Misri mpaka ukafika kwenye nyumba ya Yusuf. Wakaingia, na Yusuf akawatanguliza wazazi wake akawaweka kwenye kochi. Yaa'qub na ahali zake wakajaa furaha kwa uzuri wa mapokezi aliyi watengezea Mwenyezi Mungu katika mikono ya Yusuf. Kwani kwa hayo ukoo wote umekusanyika hapo baada ya mfarakano, na umetukuka makamu makubwa ya utukufu na hishima. Wakamuamkia maamkio yaliyo zowewa na watu tangu zamani ya kuwaamkia maraisi na watawala. Wakaonyesha unyenyekevu kwa utawala wake. Yale yalimkumbusha Yusuf ile ndoto yake ya utotoni. Akamwambia baba yake: Hii ndio tafsiri ya ndoto niliyo iota na nikakusimulia ya kwamba nimeota usingizini kuwa nyota kumi na moja na jua na mwezi zinanisujudia; ni hivi basi Mola wangu Mlezi ametimiza, na amenitukuza na amenifanyia hisani. Amedhihirisha kuwa sina makosa, na akanitoa kifungoni, na akakuleteni kutoka jangwani tukutane, baada ya Shetani kutufisidi baina yangu na ndugu zangu, akawachochea dhidi yangu. Na haya yote yasinge kuwa bila ya Mwenyezi Mungu kuyafanya. Yeye ndiye wa kupanga na kuyafanya mambo yatimie kama atakavyo. Na Yeye ndiye Mwenye kuzunguka kila kitu kwa ujuzi wake, ambaye hukumu yake ni yenye kushinda katika kila jambo na kadhiya.

101 Yusuf akamwelekea Mwenyezi Mungu akimshukuru kwa kuzihisabu neema zake juu yake, na akimwomba amzidishie fadhila zake, kwa kusema: Ewe Mola wangu Mlezi! Neema zako kwangu ni nyingi mno, na bora mno! Umenipa utawala, na nakuhimidi kwa hayo. Ukanitunukia ilimu ya kufasiri

- 102.** Hizi ni katika khabari za ghaibu tulizo kufunulia. Na hukuwa pamoja nao walipo azimia shauri yao, walipo fanya njama zao wakizua vitimbi.¹⁰²
- 103.** Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.¹⁰³
- 104.** Wala wewe huwaombi ujira kwa haya. Hayakuwa haya ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.¹⁰⁴
- 105.** Na ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazo zipitia, na hali ya kuwa wanazipuuza.¹⁰⁵
- 106.** Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina.¹⁰⁶
- 107.** Je! Wanaaminisha kuwa haitowajia adhabu ya Mwenyezi Mungu ya kuwagubika, au haitawafikia Saa ya Kiyama kwa ghafla, na hali hawatambui?¹⁰⁷
- 108.** Sema: Hii ndiyo Njia yangu - ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa kujua - mimi na wanao nifuata. Na ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika washirikina.¹⁰⁸
- 109.** Na hatukuwatuma Mitume kabla yako isipo kuwa wanaume tulio wafunulia wahyi miongoni mwa watu wa mijini. Je! Hawatembei katika ardhi wakaona jinsi ulivyo kuwa mwisho wa walio kuwa kabla yao? Na hakika nyumba ya Akhera ni bora kwa wamchao Mungu. Basi hamfahamu?¹⁰⁹

ndoto kama ulivyo nitunukia! Ewe Muumba mbingu na ardhi! Wewe ndiye uliye miliki mambo yangu yote, na Mtawala wa neema za uhai wangu na baada ya kufa kwangu! Nifungamanishe nawe kwa ulivyo waridhia Manabii wako katika Dini ya Kiislamu, na unilingize katika kundi la ulio waongoa kwenye wema miongoni mwa baba zangu, na waja wako walio wema, walio safika.

102 Ewe Nabii! Haya tuliyo kusimulia ni katika khabari zilizo pita za kale. Hazikukufikia ila kwa wahyi ulio toka kwetu. Wala wewe hukuwapo pale nduguze Yusuf walipo kuwa wakipanga njama. Wala wewe hukuwa unavijua vitimbi vyao ila kwa kusimuliwa nasi.

103 Na wapo wengi ambao tabia zao zina maradhi zinazo wazuia wasiadiki haya unayo funuliwa, hata moyo wako ukiwa una shauku namna gani waamini, au nafsi yako ikafanya juhudi gani waongoke.

104 Wala hatukusudii kwa hadithi za uwongofu unazo waeleza kuwa ndio upate malipo au manufaa. Ikiwa hawaongoki hawa usiwahuzunike. Mwenyezi Mungu atawaongoa watu wengineo. Kwani Sisi hatukuwateremshia wao tu peke yao. Na haya si chochote ila ni mawaidha, na mazingatio kwa kila aliye umbwa na Mwenyezi Mungu katika mbingu na ardhi.

105 Na dalili ni nyingi mno za kuonyesha kuwepo Muumba, na Upweke wake, na Ukamilifu wake, ziliomo katika mbingu na ardhi, ambazo wanazona watu wako, na wanazipuuza kwa inda, hawataki kuzizingatia.

106 Na kati yao wapo wenye kumsadiki Mwenyezi Mungu, wanamkubali kuwa ni Mola Mlezi, na kwamba Yeye ni Muumba wa kila kitu. Lakini imani ya wengi wao haikusimama juu ya msingi madhubuti wa Tawhid! Basi hawaukubali Upweke wa Mwenyezi Mungu kwa njia ya usafi. Lakini katika nafsi zao umo mchanganyiko wa imani unao wapelekea katika njia za washirikina, mapagani.

107 Kwani wamechukua ahadi kwa Mwenyezi Mungu asiwaadhibu, wakadhaminika isiwapate adhabu ya kuwagubika kwa nakama yake, kama ilivyo wafanyia walio watangulia kabla yao? Au Kiyama kisiwajie kwa ghafla, kikawatesa nao wameshikamana na ushirikina na ukafiri na kisha mwisho wao uwe Motoni?

108 Ewe Muhammad! Wazindue mwisho wa uwezo wako, na waonyeshe hadi ya juhudi yako, uwaambie: Huu ndio Mwendu wangu na Njia yangu. Nawaita watu wafuate Njia ya Mwenyezi Mungu. Na mimi nimethibiti katika hili jambo langu, na kadhalika anayaitia hayo kila mwenye kunifuata na akaiamini sharia yangu. Na namtakasa Mwenyezi Mungu *Subhanahu* na kila kisicho kuwa laiki yake. Wala mimi simshirikishi Yeye na kitu chochote.

109 Wala Sisi hatukuacha mtindo wetu katika kuwateuwa Mitume tulipo kuteuwa wewe, ewe Nabii! Wala hali ya kaumu yako haikuwa mbali na hali ya kaumu nyengine zilizo tangulia. Kwani hatukuwateuwa Malaika kabla yako, bali tuliwateuwa wanaume wanaadamu katika watu wa mijini, ukawateremkia Ufunuo, yaani Wahyi. Tukawatuma kuwa ni wabashiri na waonyaji. Wenye kuongoka wakawaitikia,

110. Hata Mitume walipo kata tamaa na wakaona kuwa wamekadhibishwa, hapo ikawajia nusura yetu, wakaokolewa tuwatakao. Na adhabu yetu haitowawacha kaumu ya wakosefu.¹¹⁰

111. Kwa hakika katika hadithi zao limo zingatia kwa wenye akili. Si maneno yaliyo zuliwa, bali ni ya kusadikisha yaliyo kabla yake, na ufafanuzi wa kila kitu, na ni uwongofu na rehema kwa kaumu yenye kuamini.¹¹¹

na wapotovu wakawafanyia inda! Je, watu wako wameghafilika na kweli hii? Je, wamekalishwa kitako wasiweze kutembea wakaona hao wa kale tulivyo wateketeza duniani? Na mwisho wao ni Motoni; wakaamini wenye kuamini tukawaokoa na tukawanusuru duniani. Na malipo ya Akhera ni bora kwa wenye kumkhofu Mwenyezi Mungu, wasimshirikishe wala wasimuasi. Zimeharibika akili zenu, enyi wakaidi, hata hamwezi kufikiri wala kuzingatia!

110 Ewe Muhammad! Wala usione nusura yangu inakawia, kwani nusura yangu ipo karibu na hakika inakuja. Na Sisi tuliwatuma kabla yako Mitume, na kwa mujibu wa hikima yetu msaada wetu ulikawilia. Na wao wakawa wanaendelea kukanywa na watu wao, mpaka nafsi zilipo tikisika, wakahisi kukata tamaa, nusura yetu ikawadiriki; tukawaneemesha kwa kuwaokoa na kuwaletea amani wale walio stahili kutaka uwokofu kwetu, nao ni Waumini. Tukawageuzia maovu wale walio tenda dhambi kwa inadi na wakashikilia ushirikina. Wala hapana awezae kuizuia adhabu yetu isiwafikie watu wakosefu.

111 Na Sisi tumekufunulia tuliyo kufunulia katika visa vya Manabii ili kuuthibitisha moyo wako, na iwe ni hidaya kwa watu wako. Na tumetengeneza mazingatio na waadhi wa kuwanawirisha wenye akili na busara, na wanao tambua kuwa Qur'ani ni haki na kweli. Hizi hazikuwa ni hadithi za kutunga, wala nganu za kuzua. Bali hakika ni kweli na ufunuo, wahyi, wenye kuhakikisha ukweli wa yaliyo pita katika Vitabu vya mbinguni, na walio kuja nayo Mitume wengine! Na zinabainisha yanayo hitaji kufafanuliwa katika mambo ya Dini, na zinaongoa kwendea katika Haki na Njia Iliyo Nyooka, na zinafungua milango ya rehema ya Mwenyezi Mungu ili aongoke mwenye kufuata uwongofu wake, na akawa miongoni mwa Waumini wa kweli.

Sura 13 - Ar-Ra'ad

Utangulizi

“Surat Ar-Ra’ad” ni Sura ya Madina, na imeitwa “Ra’ad” kwa kusimuliwa kwamba Radi (inamsabihi) inamtakasa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na hisabu za Aya zake ni arubaini na tatu. Imeanza Sura hii kwa kubainisha cheo cha Qur’ani Tukufu, na kwamba imeteremshwa kwa Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kisha ikabainisha uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika ulimwengu wote, na ikazindua kueleza mambo yaliyo umbwa na yenye manufaa. Kisha ikatoka kubainisha uwezo wake Mwenyezi Mungu wa kuumba, ikaingia kubainisha uwezo wake kurejesha tena na kufufua, na ujuzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu wa kila kitu, na kubainisha kudra yake ya kuadhibu duniani, na kwa hivyo yaweza kukisiwa adhabu ya Akhera. Kisha Sura hii ikaelekeza nadhari zizingatie maajabu ya ulimwengu yaliyo zagaa. Baada ya hayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amezieleza hali za watu katika kupokea kwao uwongofu wa Qur’ani. Kisha akataja sifa za Waumini katika makhusiano yao ya kibinaadamu, na tabia za makafiri na karaha yao kushikilia kutaka miujiza isiyo kuwa hii Qur’ani juu ya ubora wake wa cheo, na ikataja kejeli zao kwa Mtume wao. Na ikamueleza Mtume kuwa Mitume wa kabla yake pia walifanyiwa kejeli! Na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mwenye kusimamia vitu vyote na nafsi zote, na kwamba Yeye ni Mwenye kumlipa kila mtu kwa anavyo stahiki, na kwamba Qur’ani ndio muujiza mkubwa kabisa utakao baki mpaka Siku ya Kiyama, na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye anaye wapa nguvu Mitume wake kwa miujiza aitakayo. Na ikiwa hao washirikina wanakanya Utume wa Nabii huyu, basi Mwenyezi Mungu Mwenyewe anashuhudia ukweli wake, na Yeye ni Mwenye kutosheleza kwa hayo.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Mym Ra. (A.L.M.R.) Hizi ni Ishara za Kitabu. Na uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi ni Haki. Lakini wengi wa watu hawaamini.¹
2. Mwenyezi Mungu aliye ziinua mbingu bila ya nguzo mnazo ziona, ametawala kwenye Ufalme wake, na amefanya jua na mwezi yamt’ii, kila kimoja kinakwenda kwa kiwango maalumu. Anayapanga mambo, na anazipambanua Ishara ili mpate kuwa na yakini kukutana na Mola wenu Mlezi.²

1 “Alif Lam Mym Ra” hizi ni harufi za kutamkwa zimeanzia baadhi ya Sura za Qur’ani. Nazo zinaashiria kuwa huu ni muujiza juu ya kuwa ni harufi wanazo zitumia Waarabu katika maneno yao ya kawaida! Na harufi hizi zilikuwa zikitamkwa huwavutia Waarabu waisikilize Qur’ani! Kwani wale mapagani (washirikina) waliambizana wasiisikilize hii Qur’ani. Ikawa Waumini wakianza harufi hizi huvutia masikio ya washirikina wakawa wanasikiliza. Hakika hizo Aya au Ishara tukufu ndio hii Qur’ani, Kitabu chenye shani kubwa, uliyo teremshiwa wewe Nabii kwa haki na ukweli kutokana na Mwenyezi Mungu, aliye kuumba, na akakuteuwa. Lakini wengi wa washirikina walio yakanya yaliyo kuja ya Haki si watu wa kuikubali Haki. Bali wao wanaipinga kwa inda.

2 Hakika aliye kiteremsha hichi Kitabu ni Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye aliye zinyanyua hizi mbingu mnazo ziona zenye nyota zipitazo bila ya nguzo mnazo ziona, wala hazijui mtu ila Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa amezifunganisha hizo na ardhi kwa funganisho zisio katika ila akipenda Mwenyezi Mungu.

3. Na ndiye aliye itandaza ardhi na akaweka humo milima na mito. Na katika kila matunda akafanya dume na jike. Huufunika usiku juu ya mchana. Hakika katika haya zimo Ishara kwa watu wanao fikiri.³
4. Na katika ardhi vimo vipande vilivyo karibiana, na zipo bustani za mizabibu, na mimea mingine, na mitende yenye kuchipua kwenye shina moja na isio chipua kwenye shina moja, nayo inatiliwa maji yale yale. Na tunaifanya baadhi yao bora kuliko mengine katika kula. Hakika katika hayo zimo ishara kwa watu wanao tia mambo akilini.⁴
5. Na kama ukistaajabu, basi cha ajabu zaidi ni huo usemi wao: Ati tukisha kuwa mchanga kweli tutakuwa katika umbo jipya? Hao ndio walio mkufuru Mola wao Mlezi. Na hao ndio watao kuwa na makongwa shingoni mwao, na hao ndio watu wa Motoni. Humo watadumu.⁵
6. Na wanakuhimiza ulete maovu kabla ya mema, hali ya kuwa zimekwisha pita kabla yao adhabu za kupigiwa mfano. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye msamaha kwa watu juu ya udhalimu wao. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mkali wa kuadhibu.⁶
7. Na wale walio kufuru husema: Mbona hakuteremshiwa muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Hakika wewe ni Mwonyaji, na kila kaumu ina wa kuwaongoa.⁷

Na amedhalilisha jua na mwezi chini ya Ufalme wake na kwa ajili ya manufaa yenu. Na jua na mwezi yanazunguka kwa mpango maalumu kwa muda alio ukadiria Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la*. Na Yeye *Subhanahu* anapanga kila kitu katika mbingu na ardhi, na anakubainishieni Ishara zake za kuumba kwa kutaraji mpate kuamini kuwa Yeye ni Mmoja wa pekee.

3 Na *Subhanahu*, Mwenyezi Mungu Aliye takasika, ndiye aliye kukunjulieni ardhi, akaidhalilisha ili muweze kutembea juu yake mashariki na magharibi. Na Yeye akajaalia katika hii ardhi milima iliyo simama imara, na mito ya maji matamu inayo miminika. Na akajaalia kwa hayo maji matunda ya kabila mbali mbali yanayo zaliana, na kati ya kabila hizo namna mbali mbali, mengine matamu na mengine makali, mengine meupe, na mengine meusi. Na Yeye *Subhanahu* huufunika mchana kwa usiku. Na hakika katika huu ulimwengu na ajabu zake zimo alama wazi za kuthibitisha uwezo wa Mwenyezi Mungu na Umoja wake kwa anaye fikiri akazingatia. (*Tazama Maelezo 13:3*)

4 Na hakika hiyo ardhi nafsi yake ina maajabu. Ndani yake vipo vipande vilivyo karibiana, navyo juu ya hivyo vina udongo mbali mbali. Vingine ardhi yaabisi, na vingine vya rutba, ijapo kuwa ni udongo ule ule. Ndani yake yapo mabustani yaliyo jaa miti ya mizabibu, na ndani yake mazao mengine yanavunwa, na mitende yenye kuzaa, nayo ama iliyo kusanyika au iko mbali mbali. Na yote hayo ijapo kuwa inanyweshwa maji yale yale yanakhitalifiana kwa utamu wao. Na hakika katika ajabu hizi zipo dalili wazi za kuonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye akili ya kufikiria. (*Tazama Maelezo 13:4*)

5 Na hakika mambo ya washirikina juu ya dalili hizi ni ya ajabu. Ikiwa wewe Muhammad utastaajabia jambo, basi la ajabu ni hiyo kauli yao wanapo sema: Ati baada ya kufa, na baada ya kwisha kuwa mchanga, tutakuwa wahai tena upya? Huu ndio mtindo wa wanao mkufuru Muumba wao. Akili zao zimefungwa na upotovu. Na marejeo yao ni Motoni watakapo dumu humo; kwani hao ni wenye kukanya juu ya kuwa mwenye kuweza kuanzisha anaweza kurejesha.

6 Na huko kupita mpaka upotovu kunawapelekea kutaka wateremshiwe adhabu haraka haraka badala ya kuomba hidaya itayo waokoa. Na wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hawateremshii adhabu duniani akitaka. Na zimekwisha wapitia adhabu watu mfano wao kwa hayo, katika alio wateketeza Mwenyezi Mungu kabla yao. Lakini ni shani ya Mwenyezi Mungu kusamehe dhulma ya mwenye kutubia akarejea kwenye Haki, na kumteremshia adhabu kali anaye endelea na upotovu.

7 Na husema hao makafiri wasio amini muujiza mkubwa, yaani Qur'ani: Hebu na amteremshie Mola wake Mlezi alama ya unabii wake wa kuonekana kama kuiendesha milima akawa Mwenyezi Mungu anaonyesha wazi uhakika wa Nabii wake katika jambo hili! Na Yeye *Subhanahu* anamwambia: Hakika wewe ni Nabii wa kuwaonya kwamba kuna adhabu mbaya wakiendelea na upotovu wao. Na kila kaumu wanaye Mtume wa kuwaongoza kwenye Haki, na muujiza wa kubainisha ujumbe wake. Si wao wa kuchagua. Lao ni kujibu upinzani na kuleta mfano wake!

8. Mwenyezi Mungu anajua mimba abebayo kila mwanamke, na kinacho punguka na kuzidi matumboni. Na kila kitu kwake ni kwa kipimo.⁸
9. Yeye ndiye Mwenye kujua yanayo onekana na yasio onekana; Mkuu Aliye tukuka.⁹
10. Ni sawa anaye ficha kauli yake kati yenu na anaye idhihirisha, na anaye jibanza usiku na anaye tembea jahara mchana.¹⁰
11. Kila mtu analo kundi la malaika mbele yake na nyuma yake linamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo naf- sini mwao. Na Mwenyezi Mungu anapo watakia watu adhabu hakuna cha kuzuia wala hawana mlinzi yeyote badala yake.¹¹
12. Yeye ndiye anaye kuonyesheni umeme kwa khofu na tamaa, na huyaleta mawingu mazito.¹²
13. Na radi inamtakasa Mwenyezi Mungu kwa kumhimidi, na Malaika pia, kwa kumkhofu. Naye hupeleka mapigo ya radi yakampata amtakaye. Nao wanabishana juu ya Mwenyezi Mungu. Na Yeye ni Mwenye adhabu kali!¹³
14. Wa kuombwa kweli ni Yeye tu. Na hao wanao waomba badala yake hawawajibu chochote; bali ni kama mwenye kunyoosha viganja vyake kwenye maji ili yafike kinywani mwake, lakini hayafiki. Na maombi ya makafiri hayako ila katika upotovu.¹⁴
15. Na viliomo mbinguni na katika ardhi vinamsujudia Mwenyezi Mungu tu vikitaka

8 Aliye mpa Mtume huo muujiza mkubwa kabisa ni Yeye anaye jua kila kitu, na anazijua nafsi za binaadamu tangu kuumbwa kwao kutokana na mbegu za uzazi katika tumbo la mama mpaka wakati wa kufa kwao. Basi Yeye anajua mimba anayo ichukua kila mwanamke kama ni mume au mke, kinacho punguka tumboni na kilicho zidi wakati, mpaka utimie muda wa mimba, na mtoto akamilike kukua, azaliwe. Kila kitu kwake Yeye *Subhanahu* kina kipimo maalumu, na muda maalumu.

9 Yeye anayajua ya ghaibu tusiyo yahisi, na tunayo yashuhudia kwa ujuzi zaidi kuliko tunavyo shuhudia sisi na kuona. Na Yeye *Subhanahu* ni Mwenye shani kubwa iliyo tukuka juu ya kila kiumbe.

10 Anazijua hali zenu zote katika maisha yenu, na maneno yenu na vitendo vyenu vyote. Basi anayajua mnayo yaficha na mnayo yatangaza, vitendo na maneno. Na anajua vile mnavyo jificha usiku na kujitokeza mchana. Na yote ni sawa katika ujuzi wake.

11 Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika ndiye anaye kuhifadhini. Kila mtu anao Malaika wanao mlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu, na wanapeana zamu kumlinda mbele na nyuma yake. Na hakika Mwenyezi Mungu *Subhanahu* habadilishi hali ya watu kutoka shida kwendea neema, na kutoka nguvu wakawa dhaifu, mpaka wao wenyewe wageuze waliyo nayo kufuatana na hali wanayo iendea. Na Mwenyezi Mungu akitaka kuwateremshia watu maovu basi hawana wa kuwanusuru ataye walinda na amri yake, wala wa kuwatazamia mambo yao kuwakinga na yatayo wateremkia.

12 Na uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika ulimwengu unaonekana wazi, na athari zake zipo dhaahiri. Ni Yeye anaye kuonesheni umeme, ukakutisheni kuuona au mkakhofu isikujieni mvua wakati msio ihitaji ikakuharibieni mazao, au mkatumai kwa umeme itakuja mvua kubwa mnayo ihitajia kwa maslaha ya ukulima. Ni Yeye anaye yafanya mawingu yaliyo jaa mvua.

13 Na hakika radi zinamnyenyekea Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* kwa unyenyekevu ulio timia, mpaka ikawa sauti yake mnayo isikia ni kama kwamba inamtakasa na kumsabihii kwa kumhimidi, kumsifu na kumshukuru, kwa kuumba kwake kama ni ishara ya unyenyekevu wake. Na vile vile Roho safi msizo ziona, yaani Malaika, pia zinamtakasa Yeye. Na Yeye ndiye anaye peleka moto wa radi unao unguza ukampata amtakaye. Na juu ya kuwepo ishara hizi zinazo onekana zenye dalili ya uwezo wake *Subhanahu* wao bado wanabisha shani ya Mwenyezi Mungu Aliye takasika. Na Yeye ni Mwenye nguvu kubwa za kuvipinga vitimbi vya maadui.

14 Na hayo masanamu wanayo yaomba kwa woga na kutafuta amani badala ya Mwenyezi Mungu pekee hayawajibu wito na maombi yao. Hali yao ni kama mwenye kukunjua kiganja chake akinge maji ya kunywa na kiganja kisifike mdomoni. Na hali yao ikiwa ni hii, basi hizo dua zao haziwi ila kupotea na kukhasirika.

visitake. Na pia vivuli vyao asubuhi na jioni.¹⁵

16. Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu na ardhi? Sema: Mwenyezi Mungu. Sema: Basi je, mnawafanya wenginewe badala yake kuwa ni walinzi, nao hawajifai wenyewe kwa jema wala baya? Sema: Hebu kipofu na mwenye kuona huwa sawa? Au hebu huwa sawa giza na mwangaza? Au wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika walio umba kama alivyo umba Yeye, na viumbe hivyo vikawadanganyikia? Sema: Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu. Na Yeye ni Mmoja Mwenye kushinda!¹⁶

17. Ameteremsha maji kutoka mbinguni. Na mabonde yakamiminika maji kwa kadiri yake. Na mafuriko yakachukua mapovu yaliyo kusanyika juu yake. Na kutokana na wanavyo yayusha katika moto kwa kutaka mapambo au vyombo hutokea povu vile vile. Namna hivyo Mwenyezi Mungu ndivyo anavyo piga mifano ya Haki na baat'ili. Basi lile povu linapita kama takataka tu basi. Ama kinacho wafaa watu hubakia kwenye ardhi. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo piga mifano.¹⁷

18. Walio muitikia Mola wao Mlezi watapata wema. Na wasio muitikia, hata wangeli kuwa navyo vyote viliomo katika ardhi na mfano wa hivyo, bila ya shaka wangeli vitoa kujikombolea! Hao watapata hisabu mbaya kabisa, na makao yao ni Jahannamu. Na hapo ni pahala pabaya mno!¹⁸

15 Na vyote viliomo mbinguni na duniani, vitu, watu, majini, na Malaika, vinamnyenyekea Mwenyezi Mungu kwa matakwa yake na utukufu wake, vikitaka visitake. Hata vivuli vyao kadhaalika, vikirefuka na kufupika kwa mujibu wa nyakati za mchana adhuhuri na jioni, kwa kufuata anavyo amrisha Mwenyezi Mungu na anavyo kataza.

16 Mwenyezi Mungu amemuamrisha Nabii wake ajadiliane na washirikina kwa kuwaongoa na kuwabainisha. Akamwambia: Ewe Nabii! Waambie: Nani aliye ziumba mbingu na ardhi, naye ndiye Mwenye kuzilinda, na Mwenye kuvendesha viliomo humo? Tena uwaeleze jawabu iliyo sawa hiyo wanayo ishindania. Waambie: Huyu ni Mwenyezi Mungu anaye abudiwa kwa haki, hana mwenginewe. Basi ni waajibu wenu mumuabudu Yeye peke yake. Tena waambie: Mnazona dalili zilizo thibiti zinazo onyesha uumbaji wake kila kitu peke yake? Na juu ya hivyo mnawafanya masanamu kuwa ni miungu, bila ya kukubali kuwa Mwenyezi Mungu ni Mmoja! Na haya masanamu hayajifai wenyewe kheri wala shari! Vipi basi mnayafanya sawa na Muumba Mwenye kupanga? Nyinyi mnafanya sawa baina ya Muumba wa kila kitu na asiye miliki kitu! Mmekuwa kama anaye fanya sawa baina ya viwili vinavyo gongana! Basi hebu ni sawa baina ya mwenye kuona na asiye ona? Je, giza totoro na mwangaza unao ng'aa ni sawa? Je, usawa huo unaingia akilini mwao? Au upotovu wao umepita hadi hata wanadai kuwa hayo masanamu yao ni washirika wa Mwenyezi Mungu katika kuumba na kupanga, hata yakawadanganyikia wasijue mambo ya uumbaji, kama walivyo potea katika kuabudu? Waambie ewe Nabii! Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Muumba wa kila kiliopo. Na Yeye ni peke yake katika kuumba na kuabudiwa, Mwenye kushinda kila kitu.

17 Na hakika neema zake Mtukufu mnazona, na masanamu yenu hayana athari yoyote katika neema hizo. Yeye ndiye anaye kuteremshieni mvua kutoka kwenye mawingu, na mito na mabonde yakamiminika maji, kila kitu kwa kadiri yake aliyo ikadiria Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa ajili ya kuzalisha mimea, na matunda ya miti. Na mito inapo miminika hubeba juu yake visio kuwa na manufaa, na huwa katika hivyo vyenye nafuu hubakia, na visio na faida hupita. Mfano wa hayo ni Haki na baat'ili, kweli na uwongo. Haki hubakia na baat'ili ikapita. Na katika maadeni yanayo yayushwa kwa moto kwa kufanyia mapambo, kama dhahabu na fedha, na yanayo tumiwa kwa manufaa mengine kama chuma na shaba, kadhaalika sehemu isiyo na faida huwa juu kama povu na hutupwa. Na yenye nafuu ndio hubakia. Kadhaalika katika imani. Potovu hupita, na iliyo ya kweli hubakia. Kwa mfano kama huu Mwenyezi Mungu *Subhanahu* anabainisha ukweli wa mambo, na hupiganisha mifano hii kwa hii ili yote yabainike wazi.

18 Watu kwa mujibu wa kupokea kwao uwongofu ni mafungu mawili. Fungu moja lililo itikia wito wa Mwenyezi Mungu Muumba Mwenye kupanga. Hilo litapata malipo mema duniani na Akhera. Fungu jengine lisilo itikia wito wa Aliye waumba. Hawa watapata malipo maovu Akhera. Na lau kuwa wanamiliki kila kiliomo duniani na mfano wake mara ya pili, hawawezi kujikinga na hayo malipo maovu! Lakini

19. Je! Anaye jua ya kwamba yaliyo teremshwa kwako kutoka kwa Mola wako Mlezi ni Haki ni sawa na aliye kipofu? Wenye akili ndio wanao zingatia,¹⁹
20. Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu, wala hawavunji maagano.²⁰
21. Na wale ambao huyaunga aliyo amrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanaikhofu hisabu mbaya.²¹
22. Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao Mlezi, na wakashika Sala, na wakatoa, kwa siri na kwa uwazi, katika tulivyo wapa; na wakayaondoa maovu kwa wema. Hao ndio watakao pata malipo ya Nyumba ya Akhera.²²
23. Nayo ni Bustani za milele, wataziingia wao na walio wema miongoni mwa baba zao, na wake zao, na vizazi vyao. Na Malaika wanawaingilia katika kila mlango.²³
24. (Wakiwaambia) *Assalamu Alaikum!* Amani iwe juu yenu, kwa sababu ya mlivyo subiri! Basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya Akhera.²⁴
25. Na wale wanao vunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuzifunga, na wanakata aliyo amrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanafanya fisadi katika nchi: hao ndio watakao pata laana, na watapata Nyumba mbaya.²⁵
26. Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye, na humkunjia kwa kipimo. Na wamefurahia maisha ya dunia. Na uhai wa dunia kwa kulingana na Akhera si kitu ila

watapata kumiliki hayo? Kwa hivyo yao wao ni hisabu ya kuwaudhi, na wataishia katika Jahannamu, na huko ni pahali paovu mno pa kuishi.

19 Hakika walio ongoka na walio potoka hawawi sawa. Basi je, anaye jua ya kuwa uliyo teremshiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliye kulea akakuumba akakuteuwa kufikisha ujumbe wake, kuwa ni Haki isiyu na shaka yoyote...je huweza kuwa huyo kama aliye potea akaitupa Haki, hata akawa kama kipofu? Hakika hawatambui Haki wakazingatia utukufu wa Mwenyezi Mungu, ila watu wenye akili ya kufikiri.

20 Hao ndio wanao tambua Haki. Wao ndio wanao timiza ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu iliyo juu yao kwa muujibu wa maumbile, na kwa muujibu wa maagano yao na ahadi zao walizo fungamana nazo; wala hawavunji maagano walio fungamana nayo kwa jina la Mwenyezi Mungu baina yao na waja wenzi wao, na kwa maagano makubwa walio jifunga nayo kwa maumbile yaliyo wafanya waitambue Haki na waamini, isipo kuwa walipo jipoteza wenyewe nafsi zao.

21 Hao ni Waumini; ada yao ni mapenzi na ut'iifu. Hao wanaamini mapendo baina ya watu, na wanahurumia jamaa zao, na wanawasaidia wenzi wao katika Haki, na wao wanajua Haki ya Mwenyezi Mungu, na wanaigopa hisabu ya kuwachusha Siku ya Kiyama, na kwa hivyo wanajikinga na madhambi kwa kadri wawezavyo.

22 Na wanavumilia maudhi wakitafuta radhi za Mwenyezi Mungu iwasaidie katika Njia ya kuwania Haki. Wanashika Sala kama inavyo pasa kusafisha roho zao, na kumkumbuka Mola wao Mlezi. Na wanatoa kutokana na mali aliyo wapa Mwenyezi Mungu kisirisiri na kwa dhahiri bila ya kutaka kuonyesha watu, na kwa maovu wanao tendewa wao wanalipa mema. Na wao kwa sifa hizi watapata malipo mema kwa kukaa katika ahsani ya nyumba, nayo ndiyo Pepo.

23 Hayo ndiyo malipo mema, ya ukaazi wa moja kwa moja katika Bustani za neema. Watakuwa wao humo pamoja na wazazi wao walio kuwa njema Imani yao na a'mali yao. Pamoja nao pia watakuwa na wake zao na dhuriya zao (wazao wao). Na Roho Safi zitawasalimu na kuwaingilia kila upande.

24 Hizo Roho zitawaambia: Amani ya milele ni yenu kwa sababu ya kuvumilia kwenu maudhi, na kusubiri kwenu katika kupambana na matamano yenu. Ni mazuri mno haya malipo mnayo yapata, nayo ni kupata makaazi katika Nyumba ya Neema ya Peponi.

25 Hakika sifa za Waumini wema ni kinyume na sifa za washirikina waovu. Kwani washirikina huvunja ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyo chukua kwao kwa mujibu wa maumbile na ambayo walijifunga nayo. Kwa hivyo wamekhalifu maumbile yao na akili zao kwa kuabudu mawe yasiyo wafaa wala kuwadhuru. Na wanavunja ahadi zao wanazo fungamana na waja wenzao, tena wanakata makhusiano yao ya mapenzi na watu, na makhusiano yao na Mwenyezi Mungu. Hawazifuati amri zake, wala hawamuabudu Yeye pekee. Na wanafanya uharibifu katika ardhi kwa uvamizi na kufanya uadui na kuvuka mipaka, na kuacha kuitengeneza dunia wakanafiika nayo! Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika hapendi uchafuzi na ufisadi.

ni starehe ndogo.²⁶

27. Na wanasema walio kufuru: Kwa nini hakuteremshiwa muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu humwacha kupotea amtakaye, na humwongoa anaye elekea kwake,²⁷

28. Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!²⁸

29. Wale walio amini na wakatenda mema watakuwa na raha na marejeo mazuri.²⁹

30. Ndio kama hivi tumekutuma kwa umma ambao wamekwsihia pita kabla yao umati nyengine, ili uwasomee tunayo kufunulia, na wao wanamkufuru Rahmani, Mwingi wa Rehema! Sema: Yeye ndiye Mola wangu Mlezi. Hapana mungu isipo kuwa Yeye. Juu yake nimetegemea, na kwake ndio marejeo yangu!³⁰

31. Na kama ingeli kuwako Qur'ani ndiyo inayo endeshewa milima, na kupasuliwa ardhi, na kusemeshewa wafu, (basi ingeli kuwa Qur'ani hii). Bali mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Je, hawajajua walio amini kwamba lau kuwa Mwenyezi Mungu ange penda bila ya shaka angeli waongoa watu wote? Wala walio kufuru hawaachi kusibiwa na balaa kwa waliyo yatenda, au ikawateremkia karibu na nyumbani kwao, mpaka ifike ahadi ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi yake.³¹

26 Na ikiwa hao washirikina wanaona kuwa wao wamepewa mali mengi, na Waumini ni mafakiri, wanyonge, basi wajue kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu humpa riziki kunjufu amtakaye akizishika sababu na humdhikisha amtakaye. Basi Yeye humpa Muumini na asiye kuwa Muumini. Kwa hivyo msidhani kuwa wingi wa mali mikononi mwao kuwa ni dalili ya kuwa wao ndio wamo katika Haki. Lakini wao hufurahi kwa hayo mali walio pewa, juu ya kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu humpa dunia anaye mpenda na asiye mpenda. Na maisha ya duniani si chochote ila ni starehe duni yenye kupita!

27 Na hakika hao washirikina walio banwa na wingi wa pupa na papara husema: Je, huyu Nabii hakuteremshiwa muujiza mwengine kutoka kwa Mwenyezi Mungu? Ewe Nabii! Waambie: Sababu ya kutokuwa na Imani nyinyi si upungufu wa miujiza, bali ni upotovu tu! Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika na Aliye tukuka humwacha apotee anaye mtaka apotee, maadamu anaendelea katika njia ya upotovu. Na humwongoa aendee kwenye Haki yule ambae daima hurejea kwa Mwenyezi Mungu.

28 Na hakika hawa wanao rejea kwa Mwenyezi Mungu, na wanaikubali Haki, ndio hao walio amini ambao nyoyo zao zinatua anapo tajwa na kukumbukwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Qur'ani au vyenginevyo. Na hakika nyoyo hazitulii na kutua ila kwa kukumbukwa utukufu wa Mwenyezi Mungu na uwezo wake na kuombwa radhi yake kwa kum'ii.

29 Na hakika wanao inyenyekea Haki, na wakasimama kutenda vitendo vyema, hao watapata malipo mema, na mwisho mzuri.

30 Kama tulivyo wapelekea kaumu zilizo kwisha pita Mitume wakawaeleza yaliyo ya Haki, na wakupotea walio potea, na wakaongoka walio ongoka, na tukawapa miujiza ya kuonyesha Utume wao, kadhaalika tumekutuma wewe kwa umma wa Kiarabu na wenginewe, na kabla yao zimekwisha pita kaumu nyengine. Na muujiza wako ni hii Qur'ani uwasomee, uwawekee wazi maana yake na utukufu wake. Na wao wanaikanya rehema ya Mwenyezi Mungu walio pewa kwa kuteremshiwa Qur'ani. Basi ewe Nabii! Waambie: Mwenyezi Mungu ndiye aliye niumba, na anaye nilinda, na anaye nirehemu. Hapana mungu wa kuabudiwa kwa Haki ila Yeye. Namtegemea Yeye tu, na kwake ndio marejeo yangu na yenu.

31 Wao wanataka muujiza mwingine usio kuwa huu wa Qur'ani, juu ya ubora wa athari yake, lau kuwa kweli wanaitaka Haki na wanaikubali. Lau kuwa kuna Kitabu cha kusomwa kikaiendesha milima, kikapasua ardhi, au kikawasemeza maiti, basi Kitabu hicho kinge kuwa hii Qur'ani! Lakini watu hawa wana inda tu. Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye amri yote katika miujiza na malipo ya hao wakanyao. Na katika hayo ana uwezo kaamili. Ikiwa hao wamo katika hali hii ya inadi, basi je walio it'ii Haki hawajakata tamaa bado na kuamini kwa hawa makafiri, na wakajua kwamba kufuru yao ni kuyakataa matakwa ya Mwenyezi Mungu? Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka waongoke watu wote basi wangelingoka! Na hakika uwezo wa Mwenyezi Mungu uko dhaahiri mbele yao. Basi haziachi balaa kila

- 32.** Na hakika walifanyiwa kejeli Mitume walio kuwa kabla yako. Na nikawapururia wale walio kufuru, kisha nikawashika! Basi ilikuwaje adhabu yangu!³²
- 33.** Je! Anaye isimamia kila nafsi kwa yale iliyo yachuma...? Na wamemfanyia Mwenyezi Mungu kuwa na washirika! Sema watajeni. Au ndio mnampa khabari ya yale asiyo yajua katika ardhi; au ni maneno matupu? Bali walio kufuru wamepambiwa vitimbi vyao na wamezuiliwa njia. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha apotee basi hana wa kumwongoa.³³
- 34.** Wanayo adhabu katika maisha ya dunia, na adhabu ya Akhera hapana shaka ina mashaka zaidi. Na wala hawatakuwa na wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu.³⁴
- 35.** Mfano wa Bustani waliyo ahidiwa wachamngu, kati yake inapita mito, matunda yake ni ya daima, na pia kivuli chake. Huu ndio mwisho wa wale walio jilinda. Na mwisho wa makafiri ni Moto.³⁵
- 36.** Na tulio wapa Kitabu wanafurahia uliyo teremshiwa. Na katika makundi mengine wapo wanao yakataa baadhi ya haya. Sema: Nimeamrisha nimuabudu Mwenyezi Mungu, na wala nisimshirikishe. Kuendea kwake Yeye ndiyo ninaita, na kwake Yeye ndio marejeo yangu.³⁶
- 37.** Na ndio kama hivi tumeiteremsha Qur'ani kuwa ni hukumu kwa lugha ya Kiarabu. Na ukifuata matamanio yao baada ya kukujia ilimu hii, hutakuwa na rafiki wala mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu.³⁷

kali za kuwateketeza zikiwasibu, au kuwateremkia karibu yao, mpaka itimie ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyowapa. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu havunji miadi yake.

32 Na ikiwa hao wanao kanya wamekufanyia kejeli kwa hayo unao waitia na kwa Qur'ani, basi walifanyiwa maskhara vile vile Mitume walio tumwa kabla yako wewe, ewe Nabii. Basi usihuzunike, kwani mimi nawapa muhula tu hawa wanao kanya, kisha nitawatwaa, na hapo itakuwa adhabu kali isiyowezezana kuelezwa wala kujulikana hali yake.

33 Hakika washirikina wamefanya upumbavu katika kukanya kwao, wakamfanyia Mwenyezi Mungu washirika wa kuwaabudu. Kwani ati huyo ambaye ndiye Mwenye kuhifadhi na kuangalia kila nafsi, na kuipimia kwa kuilipa kheri na shari inayo ichuma, atakuwa wa kufananishwa na haya masanamu? Ewe Nabii! Waambie: Yaelezeni yalivyo kweli! Je, hayo masanamu ya hai? Yanaweza kujikinga na madhara? Yakiwa mawe hayanufaishi wala hayadhuru, basi mbona mnajidanganya nafsi zenu kuwa miungu hiyo ndio memwambia Mwenyezi Mungu hayo ambayo mnadhani kuwa Yeye hayajui ya ardhi hii? Au mnaikwa kwenye cheo cha kuiabudu kwa maneno yanayo toka katika ndimi zenu? Hakika iliyopo ni kuwa watu hawa wamezugwa na mazingatio yao na mawazo yao ya upotovu. Na kwa sababu hiyo wameiacha Njia ya Haki wakabaki wakitanga tanga! Na wenye kupotea kama hao, basi hawana wa kuwaongoa yeyote, kwani wameziachisha nafsi zao Njia ya Uwongofu.

34 Duniani watapata adhabu kwa kushindwa na kutekwa na kuuliwa, ikiwa Waumini watakwenda katika njia ya Haki. Na hapana shaka adhabu ya Akhera itayo wateremkia ni kali zaidi na ya kudumu zaidi. Hapana wa kuwakinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu Mwenye uwezo wa kila kitu.

35 Ikiwa hawa watapata adhabu hii, Waumini watapata Pepo na neema zake. Na hayo wamekwisha ahidiwa. Na hali ya Bustani walio ahidiwa wanao simama juu ya Haki na wakaweka kinga baina ya upotovu na Imani, ni kuwa itapitiwa chini ya miti yake maji matamu, na matunda yake ni ya daima hayasiti, na kivuli chake vilevile ni cha daima. Na haya ndiyo malipo ya wale wanao jikinga na shari. Ama makafiri wanao kanya, malipo yao ni kuingia Motoni.

36 Na wale ambao walio pewa ujuzi wa Vitabu vilivyo teremshwa ni waajibu wao wakifurahie Kitabu hichi ulicho teremshiwa wewe. Kwani hichi ni maendeleo ya ule ule ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Na wanayo ifanya dini kuwa ni sababu ya kufanya makundi mbali mbali wanayakataa baadhi ya uliyo teremshiwa kwa uadui na chuki tu. Basi ewe Nabii! Waambie: Hakika mimi sikuamrisha ila nimuabudu Mwenyezi Mungu, na nisimshirikishe katika ibada yake na kitu chochote. Na kwendea kumuabudu Yeye peke yake ndio ninalingania, ninaita, na kwake Yeye peke yake ndio marejeo yangu.

37 Na kama vilivyo teremka Vitabu vya mbinguni, tumekuteremshia wewe hii Qur'ani ili iwe ni hakimu

- 38.** Na hakika Sisi tulikwisha watuma Mitume kabla yako, na tukajaalia wawe na wake na dhuriya. Na haiwi kwa Mtume kuleta miujiza isipo kuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kila kipindi kina hukumu yake.³⁸
- 39.** Mwenyezi Mungu hufuta na huthibitisha ayatakayo. Na asili ya hukumu zote iko kwake.³⁹
- 40.** Na ikiwa tukikuonyesha baadhi ya tuliyo waahidi au tukakufisha kabla yake, juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu yetu ni hisabu.⁴⁰
- 41.** Je! Hawakuona kwamba tunaifikia ardhi tukiipunguza nchani mwake? Na Mwenyezi Mungu huhukumu, na hapana wa kupinga hukumu yake, naye ni Mwepesi wa kuhisabu.⁴¹
- 42.** Na walipanga walio kuwa kabla yao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye mipango yote. Yeye anajua inayo chuma kila nafsi. Na makafiri watajua ni ya nani nyumba ya mwisho Akhera!⁴²
- 43.** Na walio kufuru wanasema: Wewe hukutumwa. Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi, na pia yule mwenye ilimu ya Kitabu.⁴³

baina ya watu kwa yaliyo baina yao, na iwe ni hakimu wa Vitabu vilivyo tangulia kuwa ni vya kweli. Na hii Qur'ani tumeiteremsha kwa lugha ya Kiarabu. Wala usitake kuwafurahisha washirikina au *Ahli Lkitab* (watu wa Biblia), baada ya ufunuo na ilimu iliyo kufikia. Na ukitaka kuwaridhi basi hutakuwa na wa kukusaidia au kukulinda mbele ya Mwenyezi Mungu. Hapa anaambiwa Nabii, khasa wanasemewa Waumini wote. Na mahadharisho ya Waumini ni kweli kweli hivyo; na kwa Nabii ni kwa ajili ya kubainisha kuwa juu ya kuwa yeye ni mteuliwa, na mtukufu wa daraja, bado anafaa kuhadharishwa

38 Na ikiwa washirikina wanachochea watu wastaajabu kuwa wewe una wake na dhuriya, yaani wazao, na wanataka ulete muujiza mwengine usio kuwa Qur'ani, basi tulileta kabla yako Mitume wenye wake na wana vile vile. Kwani Mtume ni mwanaadamu, na ana sifa za kibinaadamu. Lakini yeye ni mbora kuliko wote. Wala Nabii hawezi kuleta muujiza kama apendavyo yeye au wapendavyo watu wake! Bali aletaye muujiza ni Mwenyezi Mungu, na Yeye ndiye anaye toa idhini. Kila kizazi katika vizazi kina amri yao aliyo waandikia Mwenyezi Mungu ya kuwasilihi. Na kila kizazi kina muujiza wake unao wanasibu. (Nabii Isa a.s. anasimuliwa katika Injili ya Yohana 5.30 kuwa alisema: *Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe.*)

39 Mwenyezi Mungu hufuta sharia na miujiza, na akaleta badala yake atakayo na akaithibitisha. Na kwake Yeye ipo asili ya Sharia zilizo thibiti zisio geuka, na ndio kwenye Umoja na asili ya fadhila zote, na mengineyo.

40 Na tukikuonyesha baadhi ya malipo au adhabu tulizo waahidi, au tukakujaalia ufe kabla ya hayo, ungesi ona kitisho kitacho washukia washirikina, na ungesi ona neema za Waumini! Lakini haya hayakukhusu wewe, juu yako wewe ni kufikisha Ujumbe tu, na kwetu Sisi peke yetu ndio hisabu.

41 Na hakika dalili za adhabu na kushindwa zipo! Hawaangalii kwamba Sisi tunazifikia nchi walizo kuwa wakizitawala zinachukuliwa na Waumini kidogo kidogo? Na kwa hivyo tunawapunguzia wao ardhi zilizo wazunguka. Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye wa kuhukumu kushinda na kushindwa, na thawabu na adhabu. Na wala hapana wa kupinga hukumu yake. Na hisabu yake ni ya mbio mbio, haihitajii kupitiwa na wakati mrefu, kwani Yeye ni Mjuzi wa kila kitu. Basi ishara zipo! (Tazama Maelezo 13:41)

42 Na walio kuwa kabla yao waliwapangia Mitume wao mipango ya uwovu. Lakini Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ndiye Mwenye mipango yote kwa makafiri walioko sasa na walio watangulia. Na watapata malipo kwa wanayo yatenda, na Yeye anayajua ayatendayo kila kiumbe. Na ikiwa wao hawajui kuwa mwisho mwema ni wa Waumini, basi Siku ya Kiyama watajua kwa kuona nani atapata mwisho mwema kwa kukaa katika Nyumba ya neema.

43 Na hadi ya ushindani wao hao wanao kanya na hawaikubali Haki ni kukwambia: Ewe Nabii! Wewe si Mtume aliye toka kwa Mwenyezi Mungu! Basi waambie: Yanitosha mimi kuwa Mwenyezi Mungu ndiye wa kunihukumia mimi nanyi, na anaye ijua hakika ya Qur'ani na ajabu zake za miujiza ya kushangaza inayo ingia katika akili ziliyo nzima.

Sura 14 - Ibrahim

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Ra. (A.L.R.) Hichi ni Kitabu tulicho kiteremsha kwako ili uwatowe watu kwenye giza uwapeleke kwenye muwangaza, kwa idhini ya Mola wao Mlezi, uwafikishe kwenye Njia ya Mwenye nguvu, Msifiwa,¹
2. Naye ni Mwenyezi Mungu ambaye ni vyake Yeye vyote viliomo katika mbingu na ardhi. Na ole wao makafiri kwa adhabu kali!²
3. Wale wanao fadhilisha maisha ya dunia kuliko Akhera, na wanawazuilia watu wasifuata Njia ya Mwenyezi Mungu, na wanataka kuipotisha. Hao wamepotelea mbali.³
4. Na hatukumtuma Mtume ila kwa ulimi wa kaumu yake ili apate kuwabainishia. Basi Mwenyezi Mungu humuacha akapotea amtakaye, na akamwongoa amtakaye. Naye ni Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima.⁴
5. Na tulimtuma Musa pamoja na miujiza yetu, tukamwambia: Watoe watu wako kwenye giza uwapeleke kwenye mwangaza. Na uwakumbushe siku za Mwenyezi Mungu. Hakika katika hayo zipo ishara kwa kila mwenye kusubiri akashukuru.⁵
6. Na Musa alipo waambia watu wake: Kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu aliyokuja alieni, pale alipo kuokoeni kutokana na watu wa Firauni walio kupeni adhabu mbaya kabisa, wakiwachinja wenenu wanaume, na wakiwawacha hai wanawake. Na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa unao toka kwa Mola wenu Mlezi.⁶

1 Alif Lam Ra - Kwa kuanzia harufi hizi ni kunabihisha muujiza wa Qur'ani, juu ya kuwa imeundwa kwa harufi hizi zinazo tumiwa kwa kusemea. Na pia kuwazindua watu waisikilize. Haya yaliyo tajwa katika Sura hii ni Kitabu kilicho teremshwa kwako wewe, Muhammad, kutokana nasi, ili uwatowe watu wote kwenye kiza cha ukafiri na ujinga waendee kwenye nuru ya Imani na ilimu, kwa kusahilishiwa na Mola wao Mlezi. Na nuru hiyo ndiye Njia ya Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda kwa kuadhibisha, na Mwenye kuhimidiwa kwa kuneemesha.

2 Njia ya Mwenyezi Mungu ambaye ndiye Mwenye kuumba na kumiliki kila kiliomo mbinguni na kwenye ardhi. Ikiwa hii ndiye hali ya Mungu wa Haki, basi makafiri, wenye kukanya, watahikikika kwa adhabu iliyoko kali.

3 Hao ndio walio khiari uhai wa duniani kuliko Akhera, na wanawazuia watu wasifuata Sharia ya Mwenyezi Mungu, na wanataka kuipotoa Sharia katika macho ya watu ili wapate kuikataa. Hao ndio wanao elezwa katika yaliyo tajwa kuwa wamepotelea mbali na Haki.

4 Na Sisi hatukumtuma Mtume yeyote kabla yako, ewe Nabii, ila kwa lugha ya kaumu yake ile tuliyo mtumia, ili apate kuwafahamisha aliyokuja nayo, na wao wayafahamu, na wayaelewe kwa wepesi. Wala si juu yake yeye kuwa lazima waongoke. Mwenyezi Mungu Mwenyewe ndiye humwacha apotee anaye mtaka kwa kuwa huyo si tayari kuitaka Haki. Na humwongoa amtakaye kwa kuwa kajitayarisha vyema kufuata Haki. Naye Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu ambaye hashindikwa atakalo, na ambaye anayapanga mambo yote kwa mahala pao. Basi haachi kupotea wala haongoi ila kwa hikima yake.

5 Na tulimtuma Musa na tukamuunga mkono kwa miujiza yetu. Tukamwambia: Watoe watu wako, Wana wa Israili, kwenye kiza cha ukafiri na ujinga uwapeleke kwenye nuru ya Imani na ilimu, na uwakumbushe vituko na nakama aliyowapelekea Mwenyezi Mungu kaumu za kabla yao. Hakika katika kukumbusha huko zipo dalili kubwa za kuthibitisha Upweke wa Mwenyezi Mungu, zinamlingania kwenye Imani kila mwenye kuthibiti kuwa na ukamilifu wa kuweza kuvumilia balaa, na kushukuru neema. Na hii ni sifa ya Muumini.

6 Ewe Nabii! Wakumbushe watu wako, huenda wakazingatia, wakati Musa alipo waambia watu wake kwa kufuata amri ya Mola wako Mlezi: Kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu kwenu, pale alipo

7. Na alipo tangaza Mola wenu Mlezi: Mkishukuru nitakuzidishieni; na mkikufuru, basi adhabu yangu ni kali.⁷

8. Na Musa alisema: Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitoshia, Msifiwa.⁸

9. Je! Hazikufikieni khabari za walio kabla yenu? Kaumu ya Nuhu, na A'adi, na Thamud, na walio baada yao, ambao hapana awajuaye ila Mwenyezi Mungu? Mitume wao waliwajia kwa hoja zilizo wazi, na wao wakarudisha mikono yao kwenye vinywa vyao, wakasema: Hakika sisi tumeyakataa hayo mliyo tumwa, na hakika sisi tuna shaka kubwa na mnayo tuitia.⁹

10. Mitume wao wakasema: Ati pana shaka na Mwenyezi Mungu, Muumba mbingu na ardhi? Yeye anakuiteni apate kukufutieni madhambi yenu, na akupeni muhula mpaka muda ulio wekwa. Wakasema: Nyinyi si chochote ila ni wanaadamu kama sisi. Mnataka kutuzuilia na waliyo kuwa wakiabudu baba zetu. Basi tulateeni hoja ilio wazi.¹⁰

11. Mitume wao wakawaambia: Sisi kweli si chochote ila ni wanaadamu kama nyinyi. Lakini Mwenyezi Mungu humfanyia hisani amtakaye katika waja wake. Wala sisi hatuwezi kuleta uthibitisho ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na juu ya Mwenyezi Mungu ndio wategemeo Waumini.¹¹

12. Na tuna nini hata tusimtegemeo Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ametuongoa kwenye Njia zetu. Na hapana shaka sisi tutayavumilia hayo maudhi mnayo tuudhi. Na

kuvueni kutokana na kaumu ya Firauni, nao wakikupatilizeni kwa adhabu ovu kabisa. Wakikufanyisheni kazi ngumu, wakiwachinja watoto wenu wa kiume, na wakiwaacha wa kike na kuwaweka katika unyonge na udhalili bila ya kuwauwa. Na mateso yote yaliyo tajwa na kuokoka ni mtihani mkubwa unao toka kwa Mwenyezi Mungu, ili upate kudhihiri uwezo wa kusubiri na kushukuru..

7 Na kumbukeni, enyi Wana wa Isra'el, pale Mola wenu Mlezi alipo kufunzeni, na akasema: Wallahi! Mkishukuru kwa neema niliyo kupeni ya kukuvueni, na mengineyo, kwa kuthibiti juu ya Imani na ut'iifu, basi hapana shaka nitakuzidishieni neema yangu. Na mkiikanya neema yangu kwa ukafiri na maasi, basi hakika nitakuadhibuni kwa adhabu ya kutia chungu. Kwani adhabu yangu ni kali kwa wanao kanya.

8 Na Musa aliwaambia watu wake walipo mpinga na kumkanya: Mkizikanya neema za Mwenyezi Mungu, wala msishukuru kwa Imani na ut'iifu, nyinyi na wote waliomo duniani, basi hakika hayo hayatamdhuru Mwenyezi Mungu chochote. Kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitoshia, hahitajii shukra za wanao shukuru. Yeye ni Mwenye kustahiki kuhimidiwa kwa dhati yake, bila ya yeyote kumhimidi.

9 Je! Hajjakufikilieni khabari za walio tangulia kabla yenu? Kaumu ya Nuhu, na A'adi, na Thamud, na kaumu nyenginezo zilizo kuja baada yao, ambao hapana anaye wajuu ila Mwenyezi Mungu kwa wingi wao. Hao walijiwa na Mitume wao kwa hoja zilizo wazi kuthibitisha ukweli wao. Na hao wakaweka mikono yao kwenye vinywa vyao, kwa mastaajabu na kukanya. Wakawaambia Mitume: Sisi tunaikataa miujiza na ishara mlizo kuja nazo. Na hakika sisi tuna shaka na hayo mnayo tuitia, mambo ya Imani na Tawhidi, ya kuwa Mungu ni mmoja. Sisi hatukuyakinika na chochote, na tuna shaka nayo!

10 Mitume wakawaambia watu wao, kwa mastaajabu, kuvunja shaka zao za kuwepo Mwenyezi Mungu na kuwa Yeye ni Mmoja peke yake: Hivyo katika kuwepo Mwenyezi Mungu Mmoja peke yake ipo shaka yoyote, na hali Yeye ndiye Muumba mbingu na ardhi bila ya kuwepo mfano wa kuigiza? Na Yeye anakuiteni apate kukusameheni baadhi ya madhambi mliyo yatenda kabla hamjaamini, na anakuakhirisheni mpaka umalizike muda wenu! Hao watu wakawaambia Mitume wao kwa kuudhi: Nyinyi si chochote ila ni watu tu, wanaadamu, kama sisi. Hamna ubora wowote wa kukufadhilisheni juu yetu hata mpewe Utume. Mnataka kwa huo wito wenu mtuzuie tusiabudu walio kuwa wakiabudu baba zetu! Basi tulateeni hoja iliyo wazi katika tunazo kwambieni.

11 Mitume wao wakawaambia: Sisi si chochote ila ni watu kama nyinyi, kama mliyvo sema. Walakini Mwenyezi Mungu huwateua awatakaye miongoni mwa waja wake akawapa Unabii na Utume. Wala hatuna sisi uwezo wa kukuleteeni hoja mnayo taka ila Mwenyezi Mungu apendavyo. Na ni juu ya Mwenyezi Mungu tu peke yake ndio wategemeo Waumini, na wantegemeo kwa kustahamia inda zenu na upinzani wenu.

juu ya Mwenyezi Mungu wategemea wanao tegemea.¹²

13. Na walio kufuru wakawaambia Mitume wao: Tutakutoeni katika nchi yetu, au mrudi katika mila yetu. Basi Mola wao Mlezi aliwaletea wahyi: Hakika tutawaangamiza walio dhulumu!¹³

14. Na tutakuwekeni katika ardhi baada yao. Haya ni kwa anaye ogopa kusimamishwa mbele yangu, na akaogopa maonyo yangu.¹⁴

15. Na wakaomba ushindi, na akashindwa kila jabari mkaidi,¹⁵

16. Ambaye nyuma yake ipo Jahannamu, na atanywishwa maji ya usaha.¹⁶

17. Awe anayagugumia, wala hawezi kuyameza. Na mauti yawe yanamjia kutoka kila upande, naye wala hafi. Na zaidi ya hayo ipo adhabu nyengine kali vile vile.¹⁷

18. Mfano wa walio mkufuru Mola wao Mlezi - vitendo vyao ni kama jivu linalo peperushwa kwa nguvu za upepo katika siku ya mdharba. Hawawezi kupata chochote katika waliyo yafanya. Huko ndiko kupotelea mbali!¹⁸

19. Huoni kuwa Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa Haki? Akitaka atakuondoeni na alete viumbe wapya!¹⁹

20. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si jambo gumu.²⁰

12 Na sisi tuna udhuru gani wa kuacha kumtegemea Mwenyezi Mungu, na Yeye ndiye aliye tuongoza kila mmoja wetu kwenye njia yake na maelekeo yake aliyo mwekea, na akamlazimisha afuate katika Dini? Na hakika sisi tunatilia mkazo tegemeo letu kwa Mwenyezi Mungu; na hapana shaka tutayavumilia maudhi yenu ya inadi na kutaka miujiza. Na juu ya Mwenyezi Mungu peke yake ndio humtegemea wanao tegemea.

13 Wakuu wa makafiri majabari wenye madaraka wakaazimia watumie nguvu walipo shindwa wote kupambana kwa hoja na dalili. Wakawaambia Mitume wao: Na liwe moja ya mawili. Ama tukutoeni katika nchi yetu, au muingie katika dini yetu. Mwenyezi Mungu akawafunulia Mitume kwa wahyi: Tutawateketeza hao makafiri kwa dhulma yao!

14 Na baada ya kuwateketeza tutakuwekeni nyinyi katika ardhi yao. Na huko kuwekwa kwa Waumini ni kweli, hakika, kwa mwenye kukhofu kusimama mbele yangu kwa ajili ya hisabu, na akakhofu ahadi yangu ya adhabu. Kwani mwenye kuingia na khofu huwa mt'ifu.

15 Hao Mitume waliomba nusura wawashinde hao watu wao wanao wapinga, baada ya kukata tamaa kuwa hawataamini tena. Mwenyezi Mungu aliwanusuru, na wakafuzu, na akakhasiri kila mwenye kiburi, akakataa kum'tii Mwenyezi Mungu, akawa shadidi wa upinzani. (Haya yaliyo wapata Mitume huwapata watu wa Mungu wote wanao wania Haki hata katika zama zetu. Ushindi wa mwisho daima anakuwa kwa walio wema, hoja kuvumilia na kuendelea na kazi ya Mungu).

16 Kushindwa kwa hao madhaalimu kunatangulia hapa duniani, na baada yake Akhera ipo adhabu ya Jahannamu. Huko watanyweshwa maji yanayo kirihhi kama usaha unao toka kwa watu wa Motoni.

17 Kunywa kwake ni taklifu, ni kama wanayagugumia, na wala hayeshi kiu, kwani hayumkini kuyaonea tamu kwa ukarhi wake na uchafu wake! Na mtu anakuwa ni kama amezungukwa na mauti kila upande kwa shida ziliopo, na wala huko katika Jahannamu hafi akapumzika na yanayo mfika, bali kila wakati anakuta adhabu nyengine kali zaidi.

18 Hakika hali za vitendo vya kheri wavifanyavyo makafiri duniani na pato lake, kwa kuwa havikujengwa juu ya msingi wa Imani, hali yake ni kama jivu. Ukaja upepo mkali ukalipeperusha siku ya kimbunga kilipo kaza. Siku ya Kiyama hawapati chochote kutokana na vitendo vyao vya namna hivyo vya duniani. Hayumkini wao kunafiika na chochote kutokana navyo, kwani hivyo havina thawabu, kama mtu mwenye vumbi linalo peperuka katika upepo asilo weza kulikamata. Na watu hawa wapotovu hujiona wenyewe ati kuwa ndio wanafanya mema, na ilhali vitendo vyao viko mbali kabisa na Njia ya Haki.

19 Ewe unae semezwa! Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi zisimame juu ya Haki kwa mujibu wa hikima yake? Na Mwenye kuweza haya basi anaweza kukuteketezeni, enyi makafiri, na akitaka akaleta viumbe wengine badala yenu nyinyi, ambao watakubali kuwepo kwake, na kwamba Yeye ni Mmoja wa pekee.

20 Na kuondoa huko na kuleta si muhali wala si uzito kwa Mwenyezi Mungu.

21. Na wote watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu. Wanyonge watawaambia walio takabari: Sisi tulikuwa wafwasi wenu; basi hebu hamtuondolei kidogo hivi katika adhabu ya Mwenyezi Mungu? Watasema: Lau Mwenyezi Mungu angeli tuongoa basi hapana shaka nasi tungeli kuongoeni. Ni mamoja kwetu tukipapatika au tukisubiri; hatuna pa kukimbilia.²¹

22. Na Shet'ani atasema itapo katwa hukumu: Hakika Mwenyezi Mungu alikuahidini ahadi ya kweli. Nami nalikuahidini; lakini sikukutumizieni. Na sikuwa na mamlaka juu yenu, isipo kuwa nilikuiteni, nanyi mkaniitikia. Basi msnilaumu mimi, bali jilaumuni wenyewe. Mimi siwezi kuwa mtetezi wenu, wala nyinyi hamwezi kuwa watetezi wangu. Hakika mimi nilikataa tangu zamani kunishirikisha na Mwenyezi Mungu. Hakika madhaalimu watakuwa na adhabu chungu.²²

23. Na walio amini na wakatenda mema wataingizwa katika Mabustani yapitayo mito kati yake, wadumu humo kwa idhini ya Mola wao Mlezi. Maamkio yao humo yatakuwa: Salaam!²³

24. Hebu hukuona vipi Mwenyezi Mungu alivyo piga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri, mizizi yake ni imara, na matawi yake yako mbinguni.²⁴

25. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake Mlezi. Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano ili wapate kukumbuka.²⁵

26. Na mfano wa neno oву ni kama mti muovu, ulio ng'olewa juu ya ardhi. Hauna imara.²⁶

21 Makafiri wote wataidhihiria kutoka makaburini kwao, waonekane kwa ajili ya kuhisabiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kudhihiri huko hakuna shaka, ni kama kwamba yametokea hivi sasa. Hapo wale wenye maoni ya kinyonge miongoni mwa wafwasi watawaambia waongozi wenye kiburi: Sisi tulikuwa wafwasi wenu katika kuwakanusha Mitume na kuwapiga vita, na kuzipuza nasaha zao. Basi je, hii leo, hamtuondolei kidogo baadhi ya adhabu? Wakubwa walio takabari watasema: Ingeli kuwa Mwenyezi Mungu ametuongoa kwenye njia ya kuokoka, na akatuwafikia, basi nasi tungeli kuongozeni na tungeli kuitieni muifuatae hiyo njia. Walakini sisi tumepotea na kwa hivyo tukakupotezeni nyinyi, yaani tumekuchagulieni tuliyo jichagulia nafsi zetu. Na leo hii sisi na nyinyi ni sawa sawa, tukisikitika au tukastahamili. Hapana pa kuikimbilia adhabu hii!

22 Mwenyezi Mungu atapo pitisha amri yake ya kuwaneemesha wat'iifu na kuwaadhibu wenye kuasi, Iblisi atawaabia wanao mfuata: Hakika Mwenyezi Mungu amekuahidini ahadi ya kweli kukhusu kufufuliwa na malipo, na ameitimiza. Na mimi nimekuahidini ahadi ya uwongo ya kwamba hakuna kufufuliwa, wala malipo, nami nimekwenda kinyume na ahadi yangu. Nami sikuwa na nguvu nanyi hata nikulazimisheni kunifuata. Lakini nimekuiteni kwa ushawishi wangu wa upotovu, nanyi mkaja mbio kunit'ii. Basi msnilaumu kwa sababu ya ushawishi wangu. Na zilaumuni nafsi zenu kwa kunitika. Wala mimi hii leo si wa kukuokoeni na adhabu. Na nyinyi hamwezi kuniokoa mimi! Mimi leo nakataa huko kunishirikisha mimi na Mwenyezi Mungu huko duniani mlipo kuwa mkinit'ii kama mtumwa anavyo mt'ii bwana wake. Hakika makafiri watapata adhabu chungu.

23 Na Akhera wataingizwa wenye kuamini, na wakatenda vitendo vyema, katika Mabustani yanayo pitiwa na mito chini ya majumba yake, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na amri yake. Maamkio yao humo kutokana na Malaika ni kufahamisha amani na utulivu.

24 Je, ewe mtu! Hujui vipi Mwenyezi Mungu alivyo fananisha neno la Haki lilio zuri, na neno la uwongo lilio baya? Amelimathili neno zuri lenye faida kuwa ni kama mti wenye manufaa. Asili yake ni mizizi iliyo shikilia baraabara kwenye ardhi na matawi yake yamenyanuka kuelekea mbinguni.

25 Hutoa matunda yake kila wakati aliyo uweka Mwenyezi Mungu yazae kwa mapendekezo ya aliye yaumba. Hivyo hivyo ndio tamshi la Tawhid, Upweke wa Mwenyezi Mungu, ni lenye kuthibiti katika moyo wa Muumini. A'mali yake inapanda kwa Mwenyezi Mungu, na inamfikilia baraka zake na thawabu zake kila wakati. Na Mwenyezi Mungu anawabainishia watu kwa mifano, anashabihisha maana kwa vitu wavijuavyo ili Waumini wawaidhike.

26 Neno la uwongo baya mfano wake ni kama mti mbaya ulio ng'olewa, umetupwa juu ya ardhi.

- 27.** Mwenyezi Mungu huwatia imara wenye kuamini kwa kauli ya imara katika maisha ya dunia na katika Akhera. Na Mwenyezi Mungu huwaacha kupotea hao wenye kudhulumu. Na Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo.²⁷
- 28.** Hebu hukuwaona wale walio badilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizo?²⁸
- 29.** Nayo ni Jahannamu! Maovu yaliyoje makaazi hayo!²⁹
- 30.** Na walimfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili wapoteze watu kwenye Njia yake. Sema: Stareheni! Kwani marejeo yenu ni Motoni!³⁰
- 31.** Waambie waja wangu walio amini, washike Sala, na watoe katika tulivyo waruzuku, kwa siri na dhaahiri, kabla haijafika Siku isiyo kuwa na biashara wala urafiki.³¹
- 32.** Mwenyezi Mungu ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi, na akateremsha maji kutoka mbinguni. Na kwa hayo akatoa matunda kuwa ni riziki yenu. Na akafanya yakutumikieni majahazi yanayo pita baharini kwa amri yake, na akaifanya mito ikutumikieni.³²
- 33.** Na akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu daima dawamu, na akaufanya usiku na mchana kwa manufaa yenu.³³
- 34.** Na akakupeni kila mlichu muomba. Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu hamwezi kuzidhibiti. Hakika mwanaadamu ni dhaalimu mkubwa, mwenye kuzikufuru neema.³⁴
- 35.** Na Ibrahim alipo sema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ujaalie mji huu uwe wa amani,

Haukusimama imara. Hali kadhaalika neno la uwongo lililo kataliwa halina uthabiti, kwa kuwa halikuungwa mkono na hoja.

27 Mwenyezi Mungu anawathibitisha imara wanao amini juu ya neno la Haki katika uhai wa duniani na Siku ya Kiyama pia. Na Mwenyezi Mungu huwabaidisha nalo neno hilo makafiri kwa kutojitengezea wenyewe. Mwenyezi Mungu hutenda atakavyo, akiwathibitisha baadhi na kuwaacha kupotea wengine. Hapana wa kumtoa kombo kwa hukumu yake, wala mwenye kuurudisha uamuzi wake!

28 Ewe msikilizaji! Hebu huwaangalii hao washirikina ambao, badala ya kushukuru neema ya Mwenyezi Mungu ya kumleta Muhammad na Dini yake, wakaingia kumkataa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na wakawasabibisha wafwasi wao kutumbukia katika nyumba ya hilaki kwa upotovu wao.

29 Na nyumba hiyo ndiyo Jahannamu wakiteswa kwa uvukuto wake. Na makaazi maovu mno ni Jahannamu.

30 Na wakamfanyia Mwenyezi Mungu Mmoja wa pekee mifano ya masanamu wakiyaabudu, kwa ajili ya kuwa natija ya vitendo vyao iwe kuwapoteza watu wasifuata Njia ya Mwenyezi Mungu! Ewe Nabii! Waambie hao walio potea: Stareheni na matamano yenu, kwani marejeo yenu ni Motoni!

31 Ewe Muhammad! Waambie waja wangu walio sadiki, wakaamini, na wakatenda mema: Shikeni Sala, na toeni baadhi ya tuliyo kuruzukuni katika njia za kheri, kwa siri na kwa dhaahiri, kabla ya kufika siku ambayo haifai kitu kupatana kibiashara wala hisani ya urafiki.

32 Ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye zianzisha mbingu na viliomo ndani yake, na ardhi na viliomo ndani yake. Na akateremsha kutoka mawinguni maji ya kumiminika. Na kwa sababu yake akakutoleeni riziki ya matunda, na mazao mengine na miti. Na Yeye akakufanyieni vyombo vya baharini vikufaeni vinakwenda na kupakia riziki zenu, na bidhaa zenu za biashara, kwa idhini yake na kutaka kwake. Na akaifanya mito ya maji matamu ikunufaisheni kwa kunywa nyinyi na kumwagia katika mashamba yenu.

33 Na akalifanya jua na mwezi yakufaeni daima dawamu, kwa mwangaza na maslahi ya mimea na wanyama. Na akajaalia usiku ukufaeni kwa kupumzika na mchana kwa kufanya kazi.

34 Na akakutengezeeni yote mnayo yahitajia katika maisha yenu ambayo anastahiki kuombwa, sawa sawa ikiwa mmemuomba au la. Na mkizihisabu neema alizo kuneemesheni Mwenyezi Mungu, hamwezi kuzidhibiti namna zake, seuze idadi yake! Hakika huyo mwenye kukanya ambaye akalipa ukafiri kuwa ni malipo ya neema alizo pewa, basi ni mwingi wa udhalimu na ukafiri!

na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu.³⁵

36. Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi. Basi aliye nifuata mimi huyo ni wangu, na aliye niasi, hakika Wewe ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.³⁶

37. Mola wetu Mlezi! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuriya zangu katika bonde lisilo kuwa na mimea, kwenye Nyumba yako Takatifu, ewe Mola wetu Mlezi, ili washike Sala. Basi zijaalie nyoyo za watu zielekee kwao, na waruzuku matunda, ili wapata kushukuru.³⁷

38. Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe unajua tunayo yaficha na tunayo yatangaza. Na hapana kitu kinacho fichikana kwa Mwenyezi Mungu katika ardhi wala katika mbingu.³⁸

39. *Alhamdulillah!* Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu aliye nipa juu ya uzee wangu Ismail na Is-haq. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye kusikia maombi.³⁹

40. Mola wangu Mlezi! Nijaalie niwe mwenye kushika Sala, na katika dhuriya zangu pia. Ewe Mola wetu Mlezi, na ipokee dua yangu.⁴⁰

41. Mola wetu! Unighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili, na Waumini, siku ya kusimama hisabu.⁴¹

42. Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayo yafanya madhaalimu. Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku yatapo kodoka macho yao.⁴²

35 Ewe Nabii! Ili watu wako wapate kuzingatia na waache ushirikina wao, wakumbushe kauli ya baba yao Ibrahim baada ya kuijenga Alkaaba. Alisema: Ewe Mola Mlezi! Ujaalie mji huu wenye Alkaaba uwe wa amani, ulindwe na wenye kudhulumu. Na unibaidishe, niwe mbali, mimi na wanangu na ibada ya masanamu.

36 Kwani masanamu yamepelekea kupotea watu wengi kwa kuyaabudu. Basi katika dhuriya zangu, wenye kunifuata mimi na wakakuabudu Wewe kwa ikhlasi, basi hao ni watu wa Dini yangu. Na wenye kuniasi kwa kushika ushirikina, basi Wewe ni Muweza wa kuwaongoa, kwani Wewe ni Mwingi na maghfira na rehema.

37 Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika mimi nimewafanyia maskani baadhi ya dhuriya zangu katika bonde la Makka ambalo halioti mimea, kwenye Nyumba yako uliyo kataza isiingiliwe na kuvunjiwa hishima yake, na ukajaalia sehemu za jirani yake ziwe na amani. Ewe Mola wetu Mlezi! Wakirimu wapate kushika Sala karibu na Nyumba hii. Na zijaalie nyoyo za bora ya watu ziwapende kwa kuizuru Nyumba yako. Na uwaruzuku matunda kwa kuletwa na hao watakao kuja, ili wapate kushukuru neema yako kwa Sala na Dua.

38 Ewe Mola wetu Mlezi! Ni sawa sawa kwako tunayo fanya siri na tunayo fanya dhaahiri. Kwani Wewe unajua maslaha yetu, na unatuonea huruma zaidi kuliko sisi wenyewe. Na hapana lifichikanalo kwako hata likiwa dogo, katika ardhi na katika mbingu. Basi hapana haja sisi ya kukuomba. Lakini juu ya hivyo tunaomba kwa kuonyesha kuwa sisi ni waja wako, twanyenyekea utukufu wako, na tunahitajia uliyo nayo, Wewe!

39 *Alhamdulillah!* Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu, aliye nipa juu ya kuwa ni mzee wa miaka mingi, na nimekwisha kata tamaa ya kuzaa, Ismail na kisha Is-haq! Hakika Mwenyezi Mungu anasikia na ananipokelea maombi yangu.

40 Ewe Mola wangu Mlezi! Niwezeshe nitimize Sala kwa inavyo takikana. Na wawezeshe watimilize kadhaalika wale walio wa kheri katika dhuriya zangu. Ewe Mola wetu Mlezi ipokee dua yangu kwa mapokezi ya kukubaliwa.

41 Ewe Mola wetu Mlezi! Nisamehe madhambi yaliyo niponyoka, na wasamehe wazazi wangu, na Waumini wote, Siku itapo hakikishwa hisabu, na baadae ikawa malipo.

42 Ewe Mtume! Wala usidhani kabisa kuwa Mola wako Mlezi ameghafilika na vitendo wafanyavyo wenye kudhulumu, kuupiga vita Uislamu na Waislamu wenyewe. Bali Yeye anaujua ukhalifu wao. Na amekadiria kuakhirisha kuwaadhibu mpaka Siku nzito. Macho yao yatabaki yamekodoka, hawawezi kuyafumba, wala kupepesa kwa kitisho watacho kiona.

- 43.** Nao wako mbioni, vichwa juu, na macho hayapepesi, na nyoyo zao tupu.⁴³
- 44.** Na waonye watu siku itapo wajia adhabu, na walio dhulumu waseme: Ewe Mola wetu Mlezi! Tuakhirishe muda kidogo tuitikie wito wako na tuwafuate Mitume. Kwani nyinyi si mliapa zamani kwamba hamtaondokewa?⁴⁴
- 45.** Na mkakaa katika maskani zile zile za walio zidhulumu nafsi zao. Na ikakudhihirikieni jinsi tulivyo watendea. Nasi tukakupigieni mifano mingi.⁴⁵
- 46.** Na kwa hakika walifanya vitimbi vyao, na vitimbi vyao anavijua Mwenyezi Mungu. Wala vitimbi vyao si vya kuondosha milima.⁴⁶
- 47.** Basi usimdhanie Mwenyezi Mungu kuwa ni mwenye kuwavunjia ahadi yake Mitume wake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushinda, na ni Mwenye kulipiza.⁴⁷
- 48.** Siku itapo geuzwa ardhi iwe ardhi nyengine, na mbingu pia. Nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye nguvu.⁴⁸
- 49.** Na utaona wakhafifu siku hiyo wamefungwa katika minyororo;⁴⁹
- 50** Nguo zao zitakuwa za lami, na Moto utazigubika nyuso zao.⁵⁰
- 51.** Ili Mwenyezi Mungu ailipe kila nafsi kwa yale iliyo yachuma. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.⁵¹
- 52.** Hili ni Tangazo liwafikie watu, liwaonye, na wapate kujua kuwa hakika Yeye ni Mungu Mmoja, na wapate kukumbuka wenye akili.⁵²

43 Nao wako mbioni kumwendea anaye wita, vichwa vyao vimeelekea juu mbinguni, macho yao hayapepesi hata wakitaka, na nyoyo zao tupu hazina wazo lolote kwa wingi wa khofu.

44 Ewe Nabii! Waeleze watu khabari za vitisho vya Siku ya Kiyama watapo sema walio zidhulumu nafsi zao kwa ukafiri na maasi: Mola wetu Mlezi, tuakhirishe adhabu, uturejeshe duniani, na utupe muhula kwa muda mdogo, walau tudiriki kuitikia wito wako wa Tawhidi na kuwafuata Mitume. Nao wataambiwa: Leo ndio mwasema haya? Na mmesahau ya kwamba mliapa nyinyi ya kuwa mkifa neema hizi hazitokuundokeeni mtao fufuliwa Siku ya Kiyama.

45 Na mkakaa duniani katika maskani zile zile za wale walio tangulia kuzidhulumu nafsi zao kwa ukafiri na maasi miongoni mwa kaumu zilizo kuwa kabla yenu. Na ikadhihiri kwenu kwa kuona mabaki ya vile tulivyo waadhibu wao, na nyinyi msiwaidhike. Na tukakuelezeni waliyo yafanya wao, na nini kilicho wafika. Nanyi msizingatie.

46 Na wakapanga hao washirikina njama zao kutaka kuvunja Daa'wa, yaani Wito. Na Mwenyezi Mungu anazijua vyema hila zao. Wala vitimbi vyao haviwezi kuiondoa Sharia iliyo thibiti imara kama milima.

47 Ewe Mtume! Usidhani kuwa Mwenyezi Mungu atawatupa Mitume wake kwa kwenda kinyume na ahadi aliyo wapa kuwa atawanusuru. Kwani Yeye daima ni Mwenye kushinda, hapana mmoja awezaye kumzuia kwa alitakalo, ni Mkali wa kulipiza kwa anaye mkanya na kumuasi.

48 Basi Mwenyezi Mungu atalipizia Siku ya Kiyama itapo geuzwa ardhi iwe ardhi nyengine sio hii ya sasa, na mbingu hali kadhaalika zigeuzwe ziwe nyengine, na viumbe watolewe makaburini mwao kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu asiye na mshirika, wala wa kumshinda.

49 Utawaona makafiri Siku ya Kiyama wamefungwa pingu pamoja na mashetani wao.

50 Ngozi zao zimepakwa lami inayo chiririka, imekuwa kama ndio nguo juu ya ngozi zao. Na moto umewapamba na huwagubika nyuso zao.

51 Wanafanyiwa hayo ili Mwenyezi Mungu apate kumlipa kila mmoja wao kwa aliyo yachuma katika dunia. Na Mwenyezi Mungu ni mwepesi wa kuhisabu Siku ya Kiyama, wala hapana kitu cha kumshughulisha.

52 Hii Qur'ani ni Tangazo la kuwanasihia na kuwaonya na kuwakhofisha adhabu ya Mwenyezi Mungu, na ili wajue ya kwamba wakikhofu wakazingatia kuwa hakika hapana mungu ila Mungu Mmoja, na ili wenye akili wakumbuke utukufu wa Mola wao Mlezi, na kwa hivyo wajitenge mbali na yale yatayo waletea hilaki.

Sura 15 - Al-Hijr

Utangulizi

Suratul Hijr ni Sura ya Makka. Nayo ina Aya 99. Imeanza kwa harufi za kutamkwa zenye kueleza kwamba Qur'ani imejengeka kwa harufi hizi hizi mnazo zitumia katika maneno yenu, na juu ya hivyo ni Muujiza kwenu, hamwezi kuleta kama hii. Kwani aliye iteremsha ni Mwenyezi Mungu, Aliye takasika, na Akatukuka. Na hizo harufi pia ni kama kuwazindua wale wanao ipuza Qur'ani, inawalingania, inawaita, waisikilize. Asaa wakanufaika, na wakahidika kumfuata Mwenyezi Mungu.

Sura hii tukufu inabainisha ili watu wazingatie yaliyo wapata kaumu zilizo tangulia, na khabari za Manabii walio kwisha pita, na yaliyo wapata kutokana na watu wao. Na pia Sura hii inaonyesha ishara za Mwenyezi Mungu katika ulimwengu, katika mbingu zilizo nyanyuliwa na zenye sayari zilizo hifadhiwa, na ardhi iliyo tandikwa, na kukunjuliwa, na milima iliyo simama imara, na pepo zenye kubeba maji, na zenye kupandishia miti. Na Sura hii pia inaashiria mpambano wa mwanzo katika maumbile ya asli baina ya maluuni Iblisi na Adam na mkewe, na kuendelea mpambano huo baina ya kheri na shari mpaka imalizike dunia. Kisha tena malipo ya shari Siku ya Kiyama, na malipo ya kheri. Na baada ya hayo Mwenyezi Mungu anasimulia visa vya Manabii wawili, Ibrahim na Luut'i, na watu wa Al Hijr. Na Sura inaeleza cheo cha Qur'ani, na hali ya washirikina katika kuipokea, na impasavyo Nabii kwa mnasaba wa ukafiri wao, navyo ni kufikisha ujumbe wake, na kuutangaza, na kumuabudu Mwenyezi Mungu mpaka ifike amri ya yakini.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Ra. (A.L.R). Hizi ni Aya za Kitabu na Qur'ani inayo bainisha.¹
2. HUENDA ikawa walio kufuru wakatamani wange kuwa Waislamu.²
3. Waache wale, na wastarehe, na iwazuge tamaa. Watakuja jua.³
4. Na hatukuuangamiza mji wowote ule ila ulikuwa na muda wake maalumu.⁴
5. Hawawezi watu wowote kuitangulia ajali yao, wala kuchelewa.⁵
6. Na walisema: Ewe uliyeteremshiwa Ukumbusho! Hakika wewe ni mwendawazimu.⁶

1 Hizi ni Aya za Kitabu cha kusomwa, chenye kubainisha, chenye kuweka wazi.

2 Watapenda, na watatamani sana makafiri wanao zikanya Aya za Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la*, watapo ona adhabu ya Siku ya Kiyama, lau kuwa walisilimu walipo kuwapo duniani, na wakafuata kwa ikhlasi Dini ya Mwenyezi Mungu.

3 Lakini sasa wamo katika kughafilika, hawazingatii adhabu itakayo wapata Akhera! Basi ukisha wafikishia ujumbe wako, na ukawaonya, waachilie mbali. Wao hawana hamu ila kula, na kustarehe kwa ladha za dunia. Tamaa ya uwongo inawazuga. Na hakika bila ya shaka yoyote watakuja jua yatakayo wapata pale watapo yaona kwa macho yao Siku ya Kiyama.

4 Na ikiwa wao wanataka wateremshiwe adhabu ya duniani, kama Mwenyezi Mungu alivyo wateketeza walio kuwa kabla yao, basi wajue kuwa Mwenyezi Mungu hauteketezi mji wowote ila kwa wakati wake maalumu.

5 Hawatangulii wala hawataakhari.

6 Na uovu wa hali yao na wingi wa kughafilika kwao hata imefika hadi kumuita Nabii wao kwa kejeli wakisema: Ewe uliye teremshiwa Kitabu cha kukumbusha! Hapana shaka kuwa wewe una wazimu moja

7. Mbona hutuletei Malaika ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli?⁷
8. Sisi hatuwateremshi Malaika ila kwa sababu ya haki, na hapo hawatapewa muhula.⁸
9. Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.⁹
10. Na hakika tulikwisha watumia Mitume mataifa ya mwanzo.¹⁰
11. Na hakuwafikia Mtume ila walimkejeli.¹¹
12. Na kama hivi ndivyo tunavyo ingiza katika nyoyo za wakosefu.¹²
13. Hawayaamini haya, na hali ya kuwa umekwisha wapitia mfano wa watu wa kale.¹³
14. Na lau tungeli wafungulia mlango wa mbingu, wakawa wanapanda,¹⁴
15. Basi wangeli sema: Macho yetu yamelevywa, bali sisi wenyewe tumerogwa.¹⁵
16. Na hakika tumeweka katika mbingu vituo vya sayari, na tumezipamba kwa wenye kuangalia.¹⁶
17. Na tumezilinda na kila shetani afukuzwaye.¹⁷
18. Isipo kuwa mwenye kusikiliza kwa kuibia, naye hufuatwa na kijinga cha moto kinacho onekana.¹⁸
19. Na ardhi tumeitandaza na humo tumeweka milima, na tumeotesha kila kitu kwa

kwa moja! Huko kumuita kuwa ndiye aliye teremshiwa Ukumbusho, yaani Mawaidha, hakukuwa ila ni kwa kejeli tu, kumfanyia maskhara.

7 Na hadi ya ukafiri wao walizidisha juu ya matusi hayo na kejeli kwa kusema: Laiti badala ya hicho Kitabu kilicho teremshwa ungesi tuletea Malaika wakawa ndio hoja yenyewe, kama wewe ni msemu kweli miongoni mwa wenye kusema kweli!

8 Na Mwenyezi Mungu aliye tukuka neno lake aliwajibu: Sisi hatuwateremshi Malaika ila huwa pamoja nao Haki ya nguvu yenye kuthibiti ambayo haina njia ya kuikataa. Basi wakiikanya huwa tena hawapewi muhula wowote, bali huteremshiwa adhabu ya hapa hapa duniani hapo hapo!

9 Na hakika, kwa ajili ya kuwa Wito wa Nabii huyu kwendea Haki udumu mpaka Siku ya Kiyama, hatuwateremshi Malaika, bali tumewateremshia hii Qur'ani ambayo kukumbusha kwake kunaendelea daima dawamu. Na Sisi ndio wenye kuilinda isiingiliwe na mageuzo na mabadiliko yoyote mpaka kusimama Kiyama.

10 Na ewe Mtume Muaminifu! Usihuzunike; kwani Sisi tuliwatuma Mitume kabla yako kwa mataifa ambao wameshikilia upotovu kama hao walivyo shikilia. Na wao wamepita pamoja na wa kale walio teketezwa kwa ukafiri wao.

11 Wala mtindo wao hao walio watangulia kwa kushikilia upotovu haukuwa ila kuwafanyia maskhara Mitume wao, Mtume baada ya Mtume, kama wanavyo kufanyia kejeli wewe! Huo ndio mtindo wa wapotovu.

12 Kama tulivyo itia Qur'ani katika nyoyo za Waumini ikaingiza mwangaza, basi kadhaalika tumeingiza upotovu katika nyoyo za walio pigwa muhuri wa ukosefu; hali ya katika nyoyo zao ikawa kinyume cha hayo. Upotovu ukatia mizizi katika roho zao.

13 Wakhalifu hao hawaamini. Na mwendo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwapa muhula mpaka waionye adhabu chungu ya Siku ya Kiyama ndio kama ulivyo kwisha tangulia.

14 Watu hao wanataka wateremshiwe Malaika. Ewe Nabii! Usidhani kuwa ndio wataamini wakiteremshiwa. Bali hata tungeli wafungulia mlango wa mbingu wakawa wanapanda huko wakaona maajabu yaliyoko, na wakawaona Malaika.

15 Bado wasingeli amini, na wangesema: Macho yetu yamefumbwa tusione, na yamefunikwa. Bali hayo si lolote ila ni uchawi tu, tumerogwa! Basi hapana faida ya ishara yoyote maadamu nyoyo zao zimeenea ukafiri.

16 Na Sisi tumeweka mbinguni sayari na nyota, kwa makundi yenye hisabu zake na yenye kukhitalifiana umbo lake na sura yake. Na kadhaalika tukazipamba kwa wenye kuziangalia kwa kutuza na kuzingatia, na kuchunguza kwazo dalili za uwezo wa Muumbaji wao.

17 Lakini Sisi tumezihifadhi na kila shetani anaye stahiki kupigwa vimondo na kufukuzwa kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

18 Na yeyote katika hao mashetani wanao jaribu kuibia kusikiliza maneno yanayo jiri baina ya wakaazi wa hizi nyota, basi Sisi tunampopoa kwa vijinga vya moto vya mbinguni vinavyo onekana wazi.

kiasi chake.¹⁹

20. Na tumekujaalieni humo vitu vya maisha yenu, na ya hao ambao nyinyi sio wenye kuwaruzuku.²⁰

21. Na hakuna chochote ila asili yake inatokana na Sisi; wala hatukiteremshi ila kwa kipimo maalumu.²¹

22. Na tunazipeleka pepo za kupandishia, na tunateremsha kutoka mbinguni maji, kisha tukakunywesheni maji hayo. Wala si nyinyi mnayo yaweka.²²

23. Na Sisi ndio tunao huisha na tunao fisha. Na Sisi ndio Warithi.²³

24. Na tunawajua walio tangulia katika nyinyi, na tunawajua walio taakhari.²⁴

25. Na hakika Mola wako Mlezi ndiye atakaye wakusanya. Hakika Yeye ni Mwenye hikima na Mjuzi.²⁵

26. Na tulimuumba mtu kwa udongo unao toa sauti, unao tokana na matope yaliyo tiwa sura.²⁶

27. Na majini tuliwaumba kabla kwa moto wa upepo umoto.²⁷

28. Na Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Hakika Mimi nitamuumba mtu kwa udongo unao toa sauti, unao tokana na matope yaliyo tiwa sura.²⁸

29. Basi nitakapo mkamilisha na nikampulizia roho yangu, basi mumwangukie kumsujudia.²⁹

19 Na tumekuumbieni ardhi, na tumekutengenezeeni mpaka ikawa kama busati lilio tandikwa, na tukaweka ndani yake milima iliyo simama imara. Na tumekuotesheeni ndani namna mbali mbali za mimea ya kukufaeni kwa uhai wenu, na tumeifanya kwa vipimo na zama maalumu katika kukua kwake, na faida yake kwa kula, na kwa kadiri ya haja zenu na kwa vipimo vyake, na sura yake kwa umbo na tabia. (*Tazama Maelezo 15:19*)

20 Na tumekujaalieni katika ardhi sababu za maisha mema. Kwani ndani yake yamo mawe ya kujengea majumba, na wanyama mnao nafika kwa nyama yao, au ngozi zao, au manyoa yao. Na yapo maadeni yanayo toka chini ya ardhi, na mengineyo. Kama ilivyo kuwa humo zipo sababu za kukuleteeni nyinyi maisha mema, basi humo pia wanapata maisha wenginewe ambao wapo chini ya mamlaka yenu, kama watoto na wafwasi, ambao Mwenyezi Mungu pekee ndiye anaye waruzuku wao na nyinyi.

21 Na hapana chochote cha kheri ila kiko kwetu kama mahodhi yaliyo jaa, nasi tunakiweka tayari na tunakitoa kwa wakati wake. Na hatuwateremshii waja wetu ila kwa kiasi maalumu, kwa mujibu tunavyo pima kwa hikima yetu ya maumbile.

22 Na Sisi tulipeleka pepo zilizo beba mvua na zilizo beba mbegu za mimea, na tukateremsha maji ya kukunywesheni. Na hayo ni kwa kufuata vile tutakavyo. Na yeyote yule hawezi kuyatenda kama hayo ila awe nayo kwake kama mahodhi au mabirika. (*Tazama Maelezo 15:22*)

23 Na ni Sisi tu peke yetu ndio tunavipa vitu vyote uhai, kisha tunavipelekea mauti, kwani uumbaji wote ni wetu.

24 Na kila mmoja wenu ana muda wake alio pimiwa. Sisi ndio tunao ujua. Tunawajua walio tangulia kwa kufa na kuwa hai, na pia wanao taakhari.

25 Na hakika walio tangulia na walio taakhari watakusanywa wakati mmoja. Na Mwenyezi Mungu atawahisabia na atawalipa. Na hayo ni kwa mujibu wa hikima yake na ujuzi wake. Na Yeye ndiye anaye itwa Mwenye hikima, Mwenye ujuzi. .

26 Na Sisi katika kuumba kwetu walimwengu katika dunia hii, tumeumba namna mbili - Tumemuumba mtu kwa udongo mkavu wenye kutoa sauti ukigongwa.

27 Na makhaluku wengine ni majini, ambao tuliwaumba mbele, alipo umbwa asili yake Iblisi kutokana na moto mkali mno unao toka katika tundu za mwili wa mtu.

28 Ewe Nabii! Kumbuka asli ya viumbe. Pale alipo sema Aliye kuumba, Mola Mlezi wa viumbe vyote, kuwaambia Malaika: Mimi nataka kumuanzisha mtu niliye muumba kutokana na udongo mkavu, wenye kutoa sauti ukigongwa, nao umebadilika rangi, na una sura.

29 Nikisha kamilisha kumuumba, na nikampulizia roho ambayo ninaimiliki, basi teremkeni kwa nyuso zenu mkimsujudia, kwa kumwamkia na kumhishimu.

- 30.** Basi Malaika wote pamoja walimsujudia,³⁰
31. Isipo kuwa Iblisi. Yeye alikataa kuwa pamoja na walio sujudu.³¹
32. (Mwenyezi Mungu) akasema: Ewe Iblisi! Una nini hata hukuwa pamoja na walio sujudu?³²
33. Akasema: Haiwi mimi nimsujudie mtu uliye muumba kwa udongo unao toa sauti, unao tokana na matope yenye sura.³³
34.(Mwenyezi Mungu) akasema: Basi toka humo, kwani hakika wewe ni maluuni!³⁴
35. Na hakika juu yako ipo laana mpaka Siku ya Malipo.³⁵
36. Akasema (Iblisi): Mola wangu Mlezi! Nipe muhula mpaka siku watapo fufuliwa.³⁶
37. (Mwenyezi Mungu) akasema: Hakika wewe ni katika walio pewa muhula.³⁷
38. Mpaka siku ya wakati maalumu.³⁸
39. Akasema: Mola wangu Mlezi! Ilivyo kuwa umenitia makosani, basi nahakikisha nitawazaini hapa duniani na nitawapoteza wote,³⁹
40. Ila waja wako walio safika.⁴⁰
41. Akasema: Hii Njia ya kujia kwangu Iliyo Nyooka.⁴¹
42. Hakika waja wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao, isipo kuwa wale wapotofu walio kufuata.⁴²
43. Na bila shaka Jahannamu ndipo pahali pao walipo ahidiwa wote.⁴³
44. Ina milango saba; na kwa kila mlango iko sehemu walio tengewa.⁴⁴

30 Wakasujudu wote kwa kuit'ii amri ya Mwenyezi Mungu.

31 Lakini Iblisi alijivuna na akakataa kuwa pamoja na Malaika walio it'ii amri ya Mwenyezi Mungu.

32 Hapo basi Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema: Ewe Iblisi! Kitu gani kilicho kupelekea hata ukaasi na usiwe pamoja na wanyenyekevu walio sujudu?

33 Iblisi akasema: Si shani yangu mimi kumsujudia mtu uliye muumba kwa udongo mkavu, wenye kutoa sauti ukigongwa, nao umegeuka rangi, wenye kutiwa sura.

34 Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: Ukiwa wewe umekuwa a'asi, umetokana na ut'iifu wangu, basi tokelea mbali kwenye Bustani hii! Kwani hakika wewe umefukuzwa kwenye rehema yangu na pahala pa hishima.

35 Na Mimi nimekwisha kuhukumia ubaidike na rehema na utukufu mpaka Siku ya Kiyama, Siku ya Hisabu na Malipo. Na hapo ndipo utapo pata adhabu, wewe na wanao kufuata.

36 Iblisi akasema, hali naye kesho kuwa ni mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu: Ewe Muumba wangu! Nipe muhula, nibakishe usinitwae mpaka Siku ya Kiyama, Siku watapo fufuliwa watu wakawa hai baada ya kufa kwao.

37 Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: Wewe utabakishwa, umepewa muhula.

38 Mpaka wakati niliyo ukadiria, ninao ujua Mimi. Na kama utavyo kuwa mrefu una kikomo.

39 Akasema Iblisi, mkhalifu, a'asi: Ewe Muumba wangu unaye nibakisha! Umenitakia upotofu, nami nikatumbukia ndani yake. Basi kwa sababu hiyo nahakikisha kuwa nitawapambia wanaadamu maovu wayaone mazuri, na nitafanya kila juhudi kuwapotoa wote!

40 Wala hawatopukana na upotovu wangu ila wale waja wako walio kufanyia ikhlasi Wewe na niso weza kuzimiliki nyoyo zao kwa zilizvyo kuwa imara kwa kukumbuka Wewe.

41 Hakika usafi wa waja walio isafia niya Dini yao ndio Njia Iliyo Nyooka, na haki yangu nisiikiuke, kwani hao siwezi kuwapotoa. (Tafsiri hii yaonyesha maneno hayo ni ya Iblisi. Lakini Tafsiri nyengine zinasema maneno hayo ni ya Mwenyezi Mungu, kwa mfano ya Abdulla Saleh, Abdulla Yusuf, Pickthall, Razi, Baidhawi, Qurtubi, Zamakhshari, Ibn Kathir, Assad.)

42 Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: Hakika waja wangu walio nisafia Mimi Dini yao wewe huna uwezo wa kuwapoteza. Lakini wapotovu, walio zama katika upotovu, walio kufuata wewe, basi hao ndio unayo madaraka juu ya nyoyo zao.

43 Na hakika Moto mkali mno ndio wameahidiwa hao wote kuwa ndiyo adhabu ya kutia uchungu.

44 Wala huo Moto mkali hauna mlango mmoja tu, bali una milango saba kwa ajili ya wingi wanao stahiki kuingia humo. Na kila mlango una kundi lake makhsusi. Na kila kundi lina cheo chake maalumu cha

45. Hakika wachamngu watakuwa katika Mabustani na chemchem.⁴⁵
46. (Wataambiwa:) Ingieni kwa salama na amani.⁴⁶
47. Na tutaondoa chuki iliyo kuwamo vifuani mwao, wawe ndugu juu ya viti vya enzi wameelekeana.⁴⁷
48. Humo hayatawagusa machofu, wala hawatatolewa humo.⁴⁸
49. Waambie waja wangu ya kwamba Mimi ndiye Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁴⁹
50. Na kwamba adhabu yangu ndio adhabu iliyo chungu!⁵⁰
51. Na uwape khabari za wageni wa Ibrahim.⁵¹
52. Walipo ingia kwake na wakasema: Salama! Yeye akasema: Hakika sisi tunakuogopeni.⁵²
53. Wakasema: Usiogope. Sisi tunakubashiria kijana mwenye ujuzi.⁵³
54. Akasema: Mnanibashiria nami uzee umenishika! Basi kwa njia gani mnanibashiria?⁵⁴
55. Wakasema: Tunakubashiria kwa haki; basi usiwe miongoni mwa wanao kata tamaa.⁵⁵
56. Akasema: Na nani anaye kata tamaa na rehema ya Mola wake Mlezi ila wale walio potea?⁵⁶
57. Akasema: Hebu nini amri yenu, enyi wajumbe?⁵⁷
58. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwa kaumu ya wakosefu!⁵⁸

kulingana na uovu wake.

45 Haya ni malipo ya wanao mfuata Shetani. Ama wale ambao Shetani kashindwa kuwapotoa, kwa kuwa wameweka kinga baina yake na nyoyo zao, hao watapata Mabustani yaliyo bora, na chemchem zinazo pita.

46 Mola wao Mlezi atawaambia: Ingieni katika Bustani hizi kwa utulivu na amani. Kwani hapana khofu juu yenu, hamhuzunikii nyakati zenu.

47 Na hakika watu wa Imani wataishi katika kheri hii na nafsi zao zimetua. Kwani tumezitoea chuki zilizo kuwamo katika nafsi hizo. Wote hao watakuwa ndugu waketi juu ya viti vya enzi zikitazamana nyuso zao kwa furaha na mahaba, wala hawawi mmoja nyuma ya mwenzie wakichunguliana visogoni.

48 Hawapatwi na machofu huko. Na hiyo ni neema ya daima, wala hawatotoka humo milele.

49 Ewe Nabii muaminifu! Wape khabari waja wangu wote kwamba Mimi ni Mwingi wa kughufria na kusamehe kwa mwenye kutubu, akaamini, na akatenda mema. Na kwamba Mimi ni Mwingi wa kuwarehemu.

50 Na wape khabari kwamba adhabu ninayo wateremshia wenye kuasi na kukufuru ni adhabu yenye kutia machungu kweli, na adhabu yoyote nyengineyo haihisabiwi kuwa ina machungu mbele ya hii.

51 Ewe Nabii! Waambie pia, katika kubainisha rehema yangu makhsusi katika dunia na adhabu yangu kwa wenye kuasi humo, khabari ya Malaika walio mfikia Ibrahim kama wageni.

52 Ewe Muaminifu! Watajia pale walipo ingia kwake, naye akawaogopa. Wao wakamwambia: Amani kwako, na tulia! Yeye akasema: Sisi tunakuogopeni, kwani mmetujia kwa ghafla, sio wakati wa dasturi wa kufika wageni, na hatujui mna nini!

53 Wakasema: Usiogope, na tuwa moyo! Kwani tunakubashiria mwana, ambaye Mwenyezi Mungu Mtukufu atampa siku zijazo za uhai wake ilimu kubwa. (*Tazama Maelezo 15:53*)

54 Akasema: Vipi mnanibashiria mtoto na hali mimi nimekwisha patikana na udhaifu wa ukongwe. Kwa njia gani, basi, mnanibashiria jambo hili la ajabu?

55 Wakasema: Sisi tunakubashiria jambo lilio thibiti, ambalo halina shaka kabisa. Basi usiwe katika wanao kata tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu.

56 Ibrahim akasema: Mimi sikati tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Kwani hawakati tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu ila walio potea wasio utambua utukufu wake na uwezo wake.

57 Alivyo kuwa kaanza kuzoana nao, alisema: Ikiwa mmenibashiria khabari hii nzuri, je mna jambo gani jenginelyo mlilo nalo baada ya haya, enyi wajumbe mlio tumwa na Mwenyezi Mungu?

58 Wakasema hakika sisi tumetumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa watu walio fanya ukhalifu

59. Isipo kuwa walio mfuata Luut'i. Bila ya shaka sisi tutawaokoa hao wote.⁵⁹
60. Ila mkewe. Tunakadiria huyo atakuwa miongoni watao bakia nyuma.⁶⁰
61. Basi wale wajumbe walipo fika kwa Luut'i,⁶¹
62. Alisema (Luut'i): Hakika nyinyi ni watu msio juulikana.⁶²
63. Wakasema: Bali sisi tumekuletea yale waliyo kuwa wakiyafanyia shaka.⁶³
64. Na tumefika kwako kwa Haki, na hakika sisi tunasema kweli.⁶⁴
65. Basi ondoka na ahli zako usiku ungalipo, nawe ufuata nyuma yao, wala yeyote kati yenu asigeuke nyuma. Na mwende mnapo amrisha.⁶⁵
66. Na tukamfunulia hukumu hiyo, ya kwamba hata wa mwisho wao hao ikifika asubuhi atakuwa kesha katiliwa mbali.⁶⁶
67. Na wakaja watu wa mji ule nao furahani.⁶⁷
68. Akasema: Hakika hawa wageni wangu, basi msinifedheheshe.⁶⁸
69. Na mcheni Mwenyezi Mungu, wala msinihizi.⁶⁹
70. Wakasema: Sisi hatukukukataza usimkaribishe yeyote?⁷⁰
71. Akasema: Hawa binti zangu, ikiwa nyinyi ni watendaji.⁷¹
72. Naapa kwa umri wako! Hakika hao walikuwa katika ulevi wao, wakihangaika ovyo.⁷²
73. Ukelele ukawatwaa wakipambaukiwa.⁷³

katika Haki ya Mwenyezi Mungu na haki ya Nabii wao, na haki ya nafsi zao wenyewe. Ukhalifu ndio mtindo wao. Watu wenyewe ni kaumu ya Luut'i. Basi tutawateketeza.

59 Wala hakusalimika na huo ukhalifu na adhabu yake ila ahli zake yeye Luut'i. Basi hao Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuamrisha tuwaokoe wote.

60 Na hatoangamia katika ahli zake ila mkewe, kwani yeye hakumfuata mumewe, bali yu pamoja na hao wakosefu ambao wanao stahiki adhabu.

61 Wale Malaika walio tumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kuteremsha yaliyo ahidiwa, walipo fika nchi ya Luut'i na watu wake.

62 Luut'i aliwaambia: Watu nyinyi sikujuini, na nafsi yangu inatishika nanyi. Naogopa msituletee balaa.

63 Wakasema: Usituogope, kwani hatukukujia kwa unalo liogopa, bali tumekujia kwa jambo la kukufurahisha, nalo ni kuwateremshia adhabu hawa watu wako walio kukadhibisha na wakawa wanaitilia shaka hiyo adhabu au wanaikanya.

64 Nasi tumekujia kwa amri iliyo thaabiti isiyu na shaka, nayo ni kuitemsha adhabu. Na kutimiza ahadi ni katika sifa yetu, kwa amri ya Mwenyezi Mungu.

65 Ilivyo kuwa adhabu itawateremkia, basi wewe na ahli zako mlio andikiwa kuokoka, tokeni baada ya kwisha ingia usiku.

66 Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* alimfunulia Luut'i kwa kumwambia: Sisi tumewahukumia na kuwakadiria wakosefu kuteketea. Watang'olewa itapoingia asubuhi, wala hatobaki hata mmoja wao.

67 Asubuhi kulipo pambazuka waliwaona Malaika kwa sura ya binaadamu wazuri. Wao wale wakawafurahia, wakaja ili wafanye nao vitendo vyao viovu, vya kuwaingilia wanaume.

68 Luut'i akaogopa wasije wakatenda vitendo vyao viovu. Akasema: Hawa ni wageni wangu, basi msinifedheheshe kwa vitendo vyenu vibaya.

69 Na mwogopeni Mwenyezi Mungu Mtukufu! Msifanye uchafu wenu, mkanipatisha hizaya na madhila mbele yao!

70 Wale wakhalifu wakasema: Kwani si tulikukataza wewe usimkaribishe mtu yeyote, na hivi sasa tena unatuzuia tusifanye nao tunayo yatamani?

71 Ili kuwanabihisha njia ya maumbile ya kisharia, Nabii wa Mwenyezi Mungu Luut'i akasema: Hawa mabinti wa mji huu, nao ni binti zangu, waoeni ikiwa mnataka kukidhi matamano yenu.

72 Ewe Nabii Muaminifu! Naapa kwa haki ya uhai wako! Hawa wamo katika mghafala, hawajui yatakayo wateremkia. Wamekuwa kama walio lewa! Hakika wao wamo katika upotovu, wanatapatapa, hawajui wapite wapi.

73 Na walipo kuwa wao wamo katika ulevi wao wa mghafala nyoyo zao na akili zao zikachotwa na

74. Na tukaigeuza nchi juu chini, na tukawanyeshea mvua ya mawe ya udongo wa Motoni.⁷⁴
75. Hakika katika hayo zipo ishara kwa waaguzi.⁷⁵
76. Na miji hii ipo kwenye njia inayo pitiwa.⁷⁶
77. Hakika katika hayo ipo ishara kwa Waumini.⁷⁷
78. Na hakika watu wa Kichakani walikuwa wenye kudhulumu.⁷⁸
79. Kwa hivyo tukawaadhibu. Na nchi mbili hizi ziko kwenye njia ilio wazi.⁷⁹
80. Na bila ya shaka wakaazi wa Hijr waliwakanusha Mitume.⁸⁰
81. Na tuliwapa ishara zetu, nao wakazipuuza.⁸¹
82. Nao walikuwa wakichonga majumba katika milima kwa amani.⁸²
83. Basi ukelele ukawatwaa asubuhi.⁸³
84. Hayakuwafaa waliyo kuwa wakiyachuma.⁸⁴
85. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ila kwa ajili ya Haki. Na hakika Kiyama kitafika. Basi samehe msamaha mzuri.⁸⁵
86. Hakika Mola wako Mlezi ndiye Muumbaji Mjuzi.⁸⁶

ukelele mkali mno wa kutisha, wakati jua lilipo chomoza.

74 Mwenyezi Mungu Aliye takasika katekeleza hukumu yake, akasema: Miji yao tukaifanya juu chini kwa kuivuruga, na tukawateremshia udongo ulio fanyika mawe ukiwateremkia kama mvua. Majumba yao yakaporomoka. Na wakitoka nje hukuta hiyo mvua ya mawe. Kwa hivyo wakawa wamezungukwa kila jiha.

75 Haya yaliyo washukia kaumu Luut'i ni alama wazi ya kuonyesha vipi Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyo timiza ahadi yake. Wajua mambo wanayatambua hayo, na wanayaelewa matokeo yake kwa alama zake, kwani kila kitendo chenye sifa ya ukosefu kina alama yake isiyo potea. Matokeo yake ni mfano wa haya, duniani na Akhera.

76 Na mabaki ya mji huu yapo yamesalia. Nayo yapo njiani katika njia inayo pitiwa na watu. Anaye taka kuwaidhika kwayo anaweza kuwaidhika.

77 Kwa kuwa mabaki yake yapo kwenye njia iliyo wazi ni dalili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kutimiza onyo lake, na Waumini wenye kut'i Haki wanatambua hayo.

78 Kama kaumu ya Luut'i walivyo kadhibisha, kadhaalika wakaazi wa Kichakani kwenye msitu wenye matunda walimkanya Mtume wao. Wakawa madhaalimu wenye kudhulumu mno katika imani yao na maingiliano yao.

79 Tukawateremshia nakama yetu. Na mabaki yao yapo njiani yanaonekana, na mpita njia akiwa ni mtu wa Imani basi anaweza kuzingatia kwayo.

80 Na kama walio tangulia hali kadhaalika wakaazi wa Hijr walimkanusha Mtume wao aliye tumwa kwao, na kwa hivyo wakawa wamewakanusha Mitume wote. Kwani ujumbe wa Mwenyezi Mungu ni mmoja. (*Tazama Maelezo 15:80*)

81 Tuliwabainishia hoja zenye kuonyesha uwezo wetu, na Utume wa Mtume wetu, nao wakayapuuza, wala wasiyafikiri.

82 Nao walikuwa watu wenye nguvu na wajenzi. Walikuwa wakijenga majumba yao katika milima na wakiichonga hiyo hiyo milima. Na wao walikuwa wakijiamini kuwa wametua na nafsi zao na mali yao.

83 Walipo kufuru na wakakanya, zikawajia sauti za kutisha, za kuonya kuteketea kwao, wakahiliki wakati wa asubuhi.

84 Wala mali waliyo yachuma na majumba waliyo yajenga hayakuwalinda na hilaki iliyo wateremkia.

85 Hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyo kati yao katika anga, na viliomo ndani yake, watu na wanyama, na mimea na visio na uhai, na vinginevyo ambavyo mwanaadamu havijui, isipo kuwa kwa uadilifu, na hikima, na maslaha ambayo hayaambatani na fisadi ya kudumu isiyo na mwisho. Na kwa hivyo basi ni lazima siku ya kukomesha shari ifike bila ya shaka yoyote. Basi ewe Nabii Mtukufu! Wasamehe hao washirikina adhabu ya duniani, na ingiana nao kwa kuwastahamia maudhi yao. Na kuwaita wito kwa hikima ni kuingiliana kwa usamehevu na upole.

86 Ewe Nabii! Mwenyezi Mungu aliye kuumba na akakulea, ni Mwenye viumbe vyote, na anajua hali yako na yao. Yeye anastahiki umtegemezee mambo yako na yao. Naye anajua maslaha yako na yao.

87. Na tumekupa Aya saba zinazo somwa mara kwa mara, na Qur'ani Tukufu.⁸⁷
88. Usivitumbulie macho yako vitu tulivyo waneemesha makundi fulani kati yao, wala usiwahuzunikie. Na wainamishie bawa lako (la huruma) Waumini.⁸⁸
89. Na sema: Hakika mimi ni mwenyaji mwenye kubainisha.⁸⁹
90. Kama hivyo tuliwateremshia walio gawa,⁹⁰
91. Ambao wakaifanya Qur'ani vipande vipande.⁹¹
92. Basi Naapa kwa Mola wako Mlezi! Tutawahoji wote,⁹²
93. Kwa waliyo kuwa wakiyatenda.⁹³
94. Basi wewe yatangaze uliyo amrisha, na jitenge na washirikina.⁹⁴
95. Hakika Sisi tunatosha kukukinga na wanao kejeli.⁹⁵
96. Hao wanao fanya kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu yupo mungu mwingine. Basi, watakuja jua!⁹⁶
97. Na Sisi tunajua kwa hakika kuwa wewe kifua chako kinaona dhiki kwa hayo wayasemayo.⁹⁷
98. Basi mtakase Mola wako Mlezi kwa kumhimidi, na uwe miongoni wanao msjudia.⁹⁸
99. Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini.⁹⁹

87 Ewe Nabii Muaminifu, tumekupa Aya saba za Qur'ani, nazo ni Sura ya Al- Fatiha unayo ikariri katika kila Sala, na humo yamo ya kutunyenyekaa na maombi ya uwongofu yaliyo kaamili. Na tumekupa Qur'ani Tukufu yote. Na ndani yake mna hoja, na miujiza. Kwa hivyo wewe una nguvu ambazo zinakufalia usamehe.

88 Ewe Mtume! Usivitazame kwa kuvitamani na kuvitaka vitu vya starehe ya dunia tulivyo wapa makafiri wa kishirikina, na Kiyahudi, na Kikristo, na Kimajusi. Kwani hivyo ni duni kwa kulinganisha na ulio pewa wewe katika kuwasiliana nasi, na Qur'ani Tukufu. Wala usiwasiikitikie kwa sababu ya kuendelea kwao na madhambi. Nawe tulia, na unyenyekee, na wachukue Waumini ulio nao kwa upole. Kwani hao ni nguvu za Haki, na watu wa Mwenyezi Mungu.

89 Ewe Nabii! Waambie makafiri wote: Mimi nakuonyeni na adhabu kali, na nakubainishieni maonyo yangu kwa hoja za kukata.

90 Haya ni kama maonyo ya walio igawanya Qur'ani wakaifanya ati ni mashairi, na ukohani, na hadithi za kale na mengineyo. Nao wasiiamini juu ya kusimama hoja juu yao.

91 Hao waliifanya Qur'ani vipande mbali mbali, nayo hali kuwa haikubali kugawika kwa umuujiza wake na ukweli wake.

92 Ikiwa hiyo hali yao, basi Wallahi kwa Aliye kuumba akakulinda na akakulea, hapana shaka tutawahisabu wote Siku ya Kiyama.

93 Kwa vitendo vyao vya kuudhi, na kufuru, na kejeli.

94 Basi wewe tangaza wito wa Haki, wala usishughulike na wayatendao washirikina na maneno yao.

95 Na hao washirikina wanao ukejeli wito wako hawatokushinda, wala hawatoweza kukuingilia kati baina yako na wito wako.

96 Hao washirikina mawazo yao yamedhoofika, ndio wakafanya kuwa Mwenyezi Mungu anao miungu mingine ya masanamu. Na watakuja jua matokeo ya ushirikina wao itapo wateremkia adhabu chungu.

97 Nasi tunajua dhiki ya moyo inayo kupata kwa wanayo yasema ya ushirikina na kejeli na dharau.

98 Ikikupata dhiki hiyo mkimbilie Mwenyezi Mungu Mtukufu umwelekee, na umt'ii na umnyenyekaa, na utake msaada kwa Sala, kwani humo ndio imo poza.

99 Na shikilia ibada ya Mwenyezi Mungu aliye kuumba, akakulinda, mpaka ifike amri ya yakini, nayo ni Kiyama na miadi.

Sura 16 - An-Nah'1

Utangulizi

Sura hii ni ya Makka, isipo kuwa Aya tatu za mwisho. Hizo ni za Madina. Idadi ya Aya zake ni mia na ishirini na nane. Sura hii tukufu imeanzia kutilia mkazo maonyo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwapa washirikina, na kubainisha uwezo wake *Subhanahu wa Taa'la* katika kutimiza ahadi hiyo, kwa dalili ya kuumba kwake mbingu na ardhi. Kisha kawabainishia watu wote kumuumba kwake ngamia, na kuotesha kwake makulima, na aliyo yaumba baharini, kama samaki wa kuliwa, na majohari ya mapambo. Kisha akaashiria yanayo wajibikia kwa neema hizo, nayo ni kumshukuru *Subhanahu*, na waajibu wa kumuabudu Yeye peke yake, na kuwakabili washirikina kwa kuwaita watambue Upweke wa Mwenyezi Mungu; na imetaja uzushi wa washirikina kuizulia Qur'ani Tukufu, na kudai kuwa hiyo ni hadithi za uwongo za kale. Kisha *Subhanahu* ameashiria adhabu ya washirikina Siku ya Kiyama na starehe za Waumini. Baadaye *Subhanahu* akataja kukanya kwa washirikina kukhusu kufufuliwa na kushikilia kwao kukanya. Naye *Subhanahu* anapinga ukafiri wao kwa kubainisha uwezo wake, na anatilia mkazo ahadi yake kwa wachamngu na vitisho vyake kwa makafiri. Kisha anakaribisha kufufuliwa kwa kueleza uwezo wake juu yao, na kuwa viumbe vyote vinamnynyekea Yeye Aliye takasika, na anabainisha kuwa ni Yeye *Subhanahu* ndiye anaye kashifu. Na anabainisha upotovu wa washirikina katika itikadi yao kuamini vitu visivyo weza kuleta nafuu wala madhara, na uovu wa maoni yao kwa wanawake wote, watoto na watu wazima. Naye *Subhanahu* ameashiria khabari za Mitume walio tangulia, akataka tuuzingatie uumbaji wake wa vitu na faida ziliomo ndani yake kwa ajili ya watu, na kutafautiana riziki, kuwa matajiri wanapewa zaidi kuliko masikini, na neema zake kwa watu kuwa wengine wanaume na wengine wanawake, na kuzaliana kwa kuoana. Naye *Subhanahu* akaingia kupiga mifano ili kueleza kudra yake. Kisha akataka watu waangalie vipi ubora wa kuumba unavyo onyesha ubora wa Mwenye kuumba na kuenea neema zake. Na vipi washirikina wanavyo zipinga neema hizi tukufu. Na baada ya kueleza matakwa ya Uislamu kuleta uadilifu, na kuunganisha udugu kwa kutimiza ahadi, na muujiza wa Qur'ani, na ukafiri wa washirikina kuikataa Qur'ani, na kuizulia uwongo, Aliye takasika ameashiria hali ya washirikina Siku ya Kiyama. Amebainisha vipi walivyo kuwa wakihalalisha na wakiharimisha bila ya hoja. Akaashiria vipi Mayahudi walivyo wakaribia washirikina, na akabainisha kuwa yapasa wasiadhibiwe isipo kuwa kwa kadiri ya walivyo tenda, na kuwa ni waajibu wa Waumini wasubiri, na washikamane na uchamngu na kufanya ihsani.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Amri ya Mwenyezi Mungu itafika tu. Basi msiihimize. Ametakasika na Ametukuka na wanayo mshirikisha nayo.¹

¹ Enyi washirikina! Kuweni na yakini kwamba aliyo kuahidini Mwenyezi Mungu kuwa yatakuwa

2. Huwateremsha Malaika na Roho kwa amri yake juu ya amtakaye katika waja wake ili nyinyi muonye kwamba hapana mungu ila Mimi, basi nicheni Mimi.²
3. Ameziumba mbingu na ardhi kwa Haki. Ametukuka na wanayo shirikisha.³
4. Amemuumba mtu kwa tone la manii. Naye mara amekuwa mshindani dhaahiri.⁴
5. Na nyama hoa amekuumbieni. Katika hao mna vifaa vya kutia joto, na manufaa mengineyo, na baadhi yao mnawala.⁵
6. Na wanakupeni furaha pale mnapo warudisha jioni na mnapo wapeleka malishoni asubuhi.⁶
7. Na hubeba mizigo yenu kupeleka kwenye miji msiyo weza kuifikia ila kwa mashaka ya nafsi. Hakika Mola wenu Mlezi ni Mpole na Mwenye kurehemu.⁷
8. Na farasi, na nyumbu, na punda ili muwapande, na kuwa ni pambo. Na ataumba msivyo vijua.⁸
9. Na ni juu ya Mwenyezi Mungu kuelekeza Njia. Na zipo njia za upotovu. Na angeli penda angeli kuongoeni nyote.⁹
10. Yeye ndiye anaye kuteremshieni maji kutoka mbinguni. Katika hayo nyinyi mnapata ya kunywa, na miti ya kulishia.¹⁰
11. Kwa hayo Yeye anaizalisha kwa ajili yenu mimea, na mizaituni, na mitende, na mizabibu, na kila namna ya matunda. Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanao

Siku ya Kiyama yapo karibu kutokea bila ya shaka. Basi msifanye maskhara kwa kuyahimiza yatokee. Mwenyezi Mungu ametakasika na kuwa na mshirika wa kuabudiwa badala yake. Na hiyo miungu mnapo mshirikisha naye haiwezi jambo lolote.

2 Mwenyezi Mungu huteremsha Malaika kwa yanayo huisha nyoyo katika Wahyi wake (ndio hiyo Roho) juu ya anaye mkhari kumpa Utume katika waja wake, ili watu wajue kwamba hapana mungu wa kuabudiwa kwa Haki ila Mimi. Basi jitengeni na yanayo nikasirisha na yatayo kuleteeni adhabu. Na shikamaneni na ut'iifu ili ukuingeni na adhabu.

3 Yeye ameumba mbingu na ardhi kwa mujibu wa hikima. Ametakasika kuwa na mshirika wa kufanya lolote katika utawala wake, au wa kuabudiwa kama Yeye.

4 Amemuumba kila mmoja katika wanaadamu kutokana na maji maji yasiyo shikamana, nayo ni manii. Kutokana na hayo ndio anakuwa mtu mwenye nguvu za kujitetea nafsi yake, mshindani na makhasimu zake, mwenye kuweka wazi hoja zake.

5 Nyi waja! Mwenyezi Mungu amekufadhilini - amekuumbieni nyama hoa, wanyama wa kufuga, kama ngamia, na ng'ombe, na kondoo, na mbuzi, ili mpate kutokana na sufi zao na manyoa yao vifaa vya kukupatieni joto kujihifadhi na baridi, na mle nyama yao mhifadhi uhai wenu.

6 Na mnapata kwao raha na furaha mnapo waona wanarejea kutoka machungani na matumbo yao na viwele vimejaa, na mnapo toka nao kwenda makondenini na machungani wakikimbilia malisha yao.

7 Na wanakubebeeni mizigo yenu mizito mpaka kwenye miji ambayo hamwezi kuifikilia bila yao isipo kuwa mziite nafsi zenu katika juhudi na mashaka makubwa. Hakika Mola wenu Mlezi aliye kutengenezeni hayo yote kwa ajili ya raha yenu bila ya shaka ni Mwingi wa upole, na Mkunjufu wa rehema kwenu.

8 Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni farasi, na nyumbu, na punda mpate kuwapanda. Na mnawafanya ni pambo la kuingiza furaha katika nyoyo zenu. Na Mwenyezi Mungu atakuja umbwa msivyo vijua sasa, katika vyombo vya kupanda na vya kukata masafa miongoni mwa alivyo msahilishia Mwenyezi Mungu binaadamu pindi akitumia akili yake na akafikiri kwayo, na akaongoka kwa kutumia kila uwezo.

9 Na juu ya Mwenyezi Mungu, kwa mujibu wa fadhila yake na rehema yake, kukuonesheni Njia Iliyo Nyooka ya kukufikisheni kwenye kheri. Na zipo njia zilizo potoka zisio fika kwenye Haki. Na lau angeli taka kukuongoeni nyote angeli kuongoeni kwenye Njia Iliyo Nyooka, lakini amekuumbieni akili ya kutambua, na matakwa ya kuelekea, na akakuacheni na khiari yenu.

10 Yeye ndiye anaye teremsha maji kutoka jiha ya mbinguni. Katika hayo mnapata kunywa, na mengine ndio inapelekea miti kumea. Nanyi hupeleka wanyama wenu wakale kwenye miti hiyo, nao wakupeni maziwa, na nyama, na sufi, na manyoa, na nywele.

fikiri.¹¹

12. Na amefanya ukutumikieni usiku na mchana, na jua na mwezi, na nyota zikutumikieni kwa amri yake. Hakika katika hayo zipo ishara kwa watu wenye akili.¹²

13. Na hivi alivyo vienezwa katika ardhi vya rangi mbali mbali. Hakika katika hayo ipo ishara kwa watu wanao waidhika.¹³

14. Yeye ndiye aliye ifanya bahari ikutumikieni, ili kutokana na humo mpate kula nyama laini, na mtoe humo mapambo mnayo yavaa. Na unaona marikebu zikikata maji humo, ili mtafute fadhila yake, na mpate kushukuru.¹⁴

15. Na kaweka katika ardhi milima ili ardhi isiyumbe yumbe nanyi. Na mito, na njia ili mpate kuongoka.¹⁵

16. Na alama nyengine. Na kwa nyota wao wanajiongoza.¹⁶

17. Ati anaye umbwa ni kama asiye umbwa? Basi hebu, hamkumbuki?¹⁷

18. Na mkizihisabu neema za Mwenyezi Mungu, hamwezi kuzidhibiti. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira, Mwenye kurehemu.¹⁸

11 Kwa maji yateremkayo mbinguni humea makulima ambayo tunakutoleeni nafaka na mizaituni, na mitende, na mizabibu na mengineyo, katika kila namna ya matunda mlayo mbali yaliyo tajwa. Hakika kuwepo vitu hivi ni alama ya kuwaongoa watu wanao nufaika kwa akili zao, wakazingatia uwezo uliyo patisha hayo.

12 Na Mwenyezi Mungu amefanya usiku ukutumikieni kwa kuufanya uwe ndio wakati wenu wa kupumzika na mchana ni muwafaka kuhangaika kwenu na kwenda kwa kazi zenu, na jua kukuleteeni joto na mwangaza, na mwezi mpate kujua idadi ya miaka na hisabu, na nyota zinazo kutumikieni kwa amri ya Mwenyezi Mungu ili mpate kujua njia katika kiza. Hakika katika hayo zipo alama na dalili kwa watu ambao wanafuika kwa akili aliyo wapa Mwenyezi Mungu.

13 Na pamoja na aliyokuumbieni Mwenyezi Mungu katika mbingu na akakutengenezeni kwa faida yenu, amekuumbieni pia juu ya ardhi wanyama namna nyingi, na mimea, na vitu visio na uhai. Na ndani ya ardhi yamo maadeni ya rangi na sura mbali mbali na faida mbali mbali. Na yote hayo kwa manufaa yenu. Hakika katika hayo zipo dalili wazi na nyingi kwa watu wanao zingatia, na wakawaidhika, na wakajua kwa hayo uwezo wa Aliye waumba, na rehema yake.

14 Ni Yeye aliye idhalilisha bahari, na akaifanya ikutumikieni, mpate kuvua na mle nyama za samaki, laini na mpya mpya. Na mtoe humo baharini mapambo kama lulu na marijani. Na ewe mwenye kuangalia ukazingatia, unaona marikebu zinavyo pita baharini zikikata maji nazo zimesheheni bidhaa na vyakula. Mwenyezi Mungu ameyadhalilisha hayo ili mnafuika nyinyi, na mtafute riziki kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu kwa njia ya biashara na nyenginezo, na mpate kumshukuru kwa aliyokuutengenezeni, na hayo ni kwa kukutumikieni nyinyi.

15 Na Mwenyezi Mungu amefanya katika ardhi milima iliyo simama imara, ili kuizuia isiyumbe yumbe. (Mwaka 1956 wataalamu wa geology, ilimu ya tabaka za ardhi, wamegundua kuwa kweli milima inasaidia kuizuia ardhi isitaharaki na kuachana. Wamevumbua kuwa mabara, continents, yamo katika kutaharaki. Kwa mfano kusini ya Amerika iliambatana na Afrika ya Magharibi, na ilisota mpaka ikafanyikana milima ya Andes. Hali kadhalika Milima ya Himalaya ikazuia kusota kwa Bara Hindi. Pia wamegundua kuwa maki ya gamba la ardhi kwa kawaida halizidi kilomita 6, lakini chini ya milima hufika hata kilomita 35. Basi ni kweli kuwa milima ni kama vizingi vya kuzuia ardhi isiyumbe, kama ilivyo sema Qur'ani miaka 1400 iliyo pita.)

Na Mwenyezi Mungu amefanya katika ardhi mito inayo pita na maji yanayo faa kunywa na kunywesha makulima, na njia zilizo tengenezwa ili mpate kuzipitia kwendea mtakako.

16 Na Mwenyezi Mungu ameweka alama za kuwaongoza watu katika safari zao kwenye ardhi, na hivyo wanapata uwongozi katika safari zao kwa nyota ambazo ameziweka mbinguni ziwaongoze wanapo kuwa gizani hawazioni alama za ardhi.

17 Hebu ni sawa kwa mwenye akili nzima baina ya Muweza na asiye weza, hata akamfanya Mwenye kuumba yote haya sawa na asiye weza kuumba kitu? Enyi washirikina! Hivyo hamzioni athari za uwezo wa Mwenyezi Mungu mkazingatia na mkamshukuru kwazo Mwenyezi Mungu?

18 Na mkitaka kuzihisabu neema za Mwenyezi Mungu juu yenu, hamwezi kuzidhibiti. Hakika Mwenyezi

19. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yaficha na mnayo yatangaza.¹⁹
20. Na wale wanao waomba wasio kuwa Mwenyezi Mungu hawaumbi kitu, bali wao wameumbwa.²⁰
21. Ni wafu si wahai, na wala hawajui watafufuliwa lini.²¹
22. Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Lakini wasio iamini Akhera nyoyo zao zinakataa, nao wanajivuna.²²
23. Hapana shaka kuwa hakika Mwenyezi Mungu anayajua wanayo yaficha na wanayo yatangaza. Kwa hakika Yeye hawapendi wanao jivuna.²³
24. Na wanapo ambiwa: Kateremsha nini Mola wenu Mlezi? Husema: Hadithi za kubuni za watu wa kale!²⁴
25. Ili wabebe mizigo yao kwa ukamilifu Siku ya Kiyama, na sehemu ya mizigo ya wale wanao wapoteza bila ya kujua. Angalia, ni maovu mno hayo wanayo yabeba!²⁵
26. Walipanga vitimbi walio kuwa kabla yao, Mwenyezi Mungu akayasukua majengo yao kwenye misingi, dari zikawaporomokea juu yao, na adhabu ikawajia kutoka wasipo kujua.²⁶
27. Kisha Siku ya Kiyama atawahizi na atasema: Wako wapi hao washirika wangu ambao kwao mkiwakutisha (Manabii) mashaka? Watasema walio pewa ilimu: Hakika leo ndiyo hizaya na adhabu itawashukia makafiri,²⁷

Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mkunjufu wa rehema. Basi tubuni kwake, na mumsafie ibada, ili apate kukusameheni na kukurehemuni.

19 Na Mwenyezi Mungu kwa ujuzi wake ulio kusanya kila kitu, anajua mnayo yaficha na mnayo yadhahirisha. Na hapana chochote kinacho fichikana kwake cha siri yenu na jahari yenu.

20 Huyu Muumba, na Mjuzi wa kila kitu, ndiye Yeye peke yake anaye stahiki kuabudiwa. Ama hayo masanamu mnayo yaabudu, hayo hayawezi kuumba chochote, hata nzi. Bali hayo yenyewe yameumbwa, na pengine mmeyaunda nyinyi wenyewe kwa mikono yenu.

21 Na hayo ni vitu visivyo na roho kama maiti, hayana hisiya yoyote, wala hayataharaki, wala hayajui Kiyama kitakuja lini, wala lini watafufuliwa hao wanao yaabudu. Wala si laiki yenu, enyi wenye akili, baada ya haya mkadhani kuwa yatakufaeni kitu hata mkayashirikisha na Mwenyezi Mungu katika kuyaabudu.

22 Na imekwisha wekwa wazi kwa kila dalili kwamba hakika Mungu wenu anaye pasa mumuabudu peke yake ni Mungu Mmoja ambaye hana mshirika wake. Na juu ya hayo wale wasio amini kufufuliwa na kuhisabiwa, nyoyo zao zinakataa Upweke wake. Kiburi chao kinawazuia kufuata Haki na kuit'ii.

23 Hapana shaka kwamba Mwenyezi Mungu anayajua wanayo yaficha na wanayo yatangaza, ikiwa ni itikadi au maneno au vitendo. Naye atawahisabu kwa yote hayo, na atawaadhibu kwa kiburi chao. Kwani hakika Yeye *Subhanahu* hawapendi wanao jivuna hata hawataki kusikia Haki na kuifuata.

24 Na wakiulizwa hao makafiri wanao jivuna: Mola wenu Mlezi kamteremshia nini Muhammad? Wao hujibu kwa inda: Hayo anayo dai kuwa Mwenyezi Mungu kamteremshia si chochote ila uzushi na upuuzi walio tunga watu wa zamani naye akayanukulu na akawa anayakariri tu.

25 Wanasema hayo ili wawazuie watu wasimfuate Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na mwisho wa kuishia mambo yao ni kuwa wataadhibiwa Siku ya Kiyama kwa adhabu ya upotovu wao kwa ukamilifu, na adhabu ya baadhi ya watu walio kuwa wakiwakhadaa na kuwadanganya mpaka wakapotea bila ya ilimu wala kuchungua! Zingatia, ewe mwenye kusikia, kwa huu uovu wa madhambi wanayo yafanya, vipi ukali wa adhabu watayo pata.

26 Na hawa makafiri wenye kiburi walitanguliwa na wengine mfano wao. Walipanga njama zao kuwapangia Manabii wao, na wakafanya hila kuwapoteza watu. Na Mwenyezi Mungu alizibomoa njama zao, akaiharibu miji yao. Akawateremshia adhabu katika dunia ambayo hawakuitaraji.

27 Na kisha huko Akhera watapo fufuliwa watu na wakahisabiwa kwa vitendo vyao, Mwenyezi Mungu atawasimamisha msimamo wa hizaya na fedheha, atapo wafedhehi na afichue waliyo kuwa wakiyaficha vifuani mwao. Atawaambia: Wako wapi hao miungu mliyo ifanya kuwa ni washirika wangu kwa kuwaabudu? Nanyi kwa ajili yao mlikuwa mkinipiga vita Mimi na Mitume wangu! Wako wapi wapate

28. Ambao Malaika waliwafisha nao wamejidhulumu nafsi zao! Basi watasalimu amri, waseme: Hatukuwa tukifanya uovu wowote. (Wataambiwa): Kwani! Hakika Mwenyezi Mungu anajua sana mliyo kuwa mkiyatenda.²⁸
29. Basi ingieni milango ya Jahannamu, humo mdumu. Ni maovu mno makaazi ya wafanyao kiburi!²⁹
30. Na wataambiwa walio mcha Mungu: Mola wenu Mlezi kateremsha nini? Watasema: Kheri. Walio fanya wema katika dunia hii watapata wema. Na nyumba ya Akhera ni bora zaidi, na njema mno nyumba ya wachamngu.³⁰
31. Bustani za milele wataziingia; iwe inapita kati yake mito. Humo watapata watakacho. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu awalipavyo wenye kumcha.³¹
32. Wale ambao Malaika huwafisha katika hali njema, wanawaambia: Amani iwe juu yenu! Ingieni Peponi kwa sababu ya yale mliyo kuwa mkiyatenda.³²
33. Wanangojea jengine hawa ila Malaika wawafikie, au iwafikie amri ya Mola wako Mlezi? Kama hivyo walitenda walio kuwa kabla yao. Na Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu, lakini walijidhulumu wenyewe.³³
34. Basi ukawafikia uovu wa waliyo yatenda, na waliyo kuwa wakiyakejeli

kukuungeni mkono, kama mlivyo kuwa mkidai? Hawatoweza kujibu! Na hapo tena wale wanao ijua Haki, miongoni mwa Manabii, na Waumini, na Malaika, watasema: Leo ndiyo hizaya na adhabu mbaya kabisa zitawashukia makafiri!

28 Hizaya itawashukia makafiri walio endelea na ukafiri wao mpaka Malaika walipo watoa roho, nao wamejidhulumu nafsi zao kwa ushirikina na kutenda maovu, na wakasalimu amri tena baada ya inadi ndefu walipo jua hakika ya makosa yao. Wakasema uwongo kwa jinsi walivyo shituka: Hatukuwa duniani tukifanya maasi yoyote! Malaika na Manabii watawaambia: Hasha! Hakika nyinyi ni waongo, bali mmetenda maasi maovu kabisa! Na Mwenyezi Mungu, *Subhanahu*, anajua vyema kila dogo na kubwa mlilo kuwa mkilitenda katika dunia yenu. Hakukuleteni faida yoyote huko kukataa kwenu!

29 Na baada ya hayo wataambiwa: Mwisho wenu ni kuingia Motoni, na adhabu ya huko ni ya milele, haikatiki! Na mbaya mno nyumba ya Jahannamu kuwa ni makaazi ya kila mwenye kutakabari akakataa kufuata Haki na Imani ya Mwenyezi Mungu na Mitume wake.

30 Na walio muamini Mwenyezi Mungu na wakajikinga na kila linalo mghadhibisha Yeye ikiwa neno, au kitendo, au itikadi, wataambiwa: Mola wenu Mlezi kamteremshia nini Mtume wake? Wao watasema: Amemteremshia Qur'ani...ndani yake mna kheri ya duniani na Akhera kwa watu wote, na kwa hivyo wakawa miongoni mwa watu wema. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* huwalipa wema kwa maisha mazuri katika uhai huu wa duniani. Na pahala pao Akhera ni bora na pazuri zaidi kuliko waliyo yapata duniani. Na nyumba watayo ikaa wachamngu Akhera ni hadi ya raha yake!

31 Nazo ni Bustani madhubuti za kudumu, zenye kupitiwa na mito chini ya majumba na miti yake. Na hao watapata kila neema waipendayo. Na mfano kama huu ndio malipo ya mema anayo walipa Mwenyezi Mungu wachamngu wote wanao muamini, na wakajikinga na yanayo mkasirisha, na wakavifanya vyema vitendo vyao.

32 Na ndio hao Malaika huzichukua roho zao na hali wamesafika na uchafu wa ushirikina na maasi. Na Malaika watawaambia kwa kuwatuza: Amani kwenu itokayo kwa Mwenyezi Mungu! Baada ya hii leo hamtopata la karaha. Na ifurahieni Pepo mtakayo ingia kwa sababu ya vitendo vyema mlivyo vitanguliza katika dunia yenu.

33 Hao ndio wachamngu walio jitengenezea Akhera yao. Na hayo ndiyo malipo yao. Ama washirikina kwa sababu ya inadi yao na kubakia kwao kwenye ushirikina wao, hawataraji ila Malaika waje kunyakua roho zao nao wamezidhulumu nafsi zao kwa ushirikina na vitendo vya shari. Na itawajia adhabu ya Mola wako Mlezi iwateketeze wote. Na kama walivyo fanya makafiri hawa, basi walikwisha wafanyia Manabii wao wale walio watangulia, na Mwenyezi Mungu akawaadhibu kwa vitendo vyao. Wala Yeye hakuwadhulumu pale alipo waadhibu, lakini wao wenyewe walizidhulumu nafsi zao walipo zitia katika adhabu kwa ukafiri wao.

yakawazunguka.³⁴

35. Na washirikina wanasema: Mwenyezi Mungu angeli taka tusingeli abudu chochote badala yake, sisi wala baba zetu, wala tusingeli harimisha chochote bila ya Yeye. Kama hivyo walifanya walio kuwa kabla yao. Basi lipo lolote juu ya Mitume isipo kuwa kubalighisha kwa uwazi?³⁵

36. Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo alio waongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao ulio wathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhii, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanao kanusha.³⁶

37. Hata ukiwa na pupa ya kutaka kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu hamwongoi yule anaye shikilia kupotea. Wala hawatapata wa kuwanusuru.³⁷

38. Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa viapo vyao kwamba Mwenyezi Mungu hatomfufua aliye kufa. Kwani! Ni ahadi iliyo juu yake kikweli; lakini watu wengi hawajui.³⁸

39. Ili kuwabainishia yale waliyo khitalifiana, na ili wajue walio kufuru kwamba wao walikuwa ni waongo.³⁹

34 Yakawasibu malipo ya maovu waliyo yatenda, na adhabu waliyo kuwa wakiikanya na kuikejeli ikawazunguka.

35 Na washirikina wakasema kwa inda na ukosefu: Lau kama Mwenyezi Mungu angeli penda tumuabudu Yeye tu peke yake na tumt'ii kwa anayo tuamuru, basi tusingeli muabudu mwenginewe, wala tusingeli harimisha sisi wenyewe kitu asicho harimisha Yeye kama *Bahira na Saiba*. Na hii ni hoja potovu wanayo itafutia njia katika ukafiri wao. Na makafiri walio kwisha tangulia walitoa hoja kama hizo, baada ya kuwapelekea Mitume wetu, wakaamrisha Tawhidi (kumuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja), na kumt'ii Yeye, na wakawakataza ushirikina na kuharimisha asivyo harimisha Mwenyezi Mungu. Hoja ikasimama dhidi yao. Na Mitume wetu wakatimiza tuliyo waamrisha wayafikishe. Na juu yetu kuwahisabu wao. Na Mitume hawana jukumu zaidi ya hayo.

36 Na kila umma tuliwapelekea Mtume awaambie: Muabuduni Mwenyezi Mungu peke yake. Na jitengeni na kila jabari mharibifu. Na wafikishe ujumbe, na uwaongoze. Basi kikundi kikasiliza uwongozi na kikafuata, na Mwenyezi Mungu akakiongoa kwa kuwa kilijitayarisha vizuri kufuata Njia Iliyo Nyooka. Na kikundi kingine kikapuza kusikia Haki, kikastahiki kwenda njia potovu, na Mwenyezi Mungu akakipelekea adhabu. Na ikiwa nyinyi, washirikina wa Makka, mna shaka na haya, basi tembeeni katika nchi za karibu nanyi, muangalie, mzingatie nini kilicho washukia wanao kanusha, kina A'ad na Thamud na Kaumu Luut'i. Na vipi ilikuwa khasara yao na hilaki yao katika mwisho wao!

37 Ewe Nabii! Ikiwa una hamu mno ya kuwaongoa washirikina katika watu wako, kwa kutumia ukomo wa juhudi yako, basi usihiliki nafsi yako kwa huzuni ikiwa hayo uyatakayo hayawi. Kwani hao wamekwisha milikiwa na matamania. Na Mwenyezi Mungu hawalazimishi kuongoka walio khiari upotovu na wakaushikilia, kwani Yeye huwacha wajichagulie wenyewe, nao watapata malipo yao, nayo ni adhabu kubwa. Na wala hawatapata Siku ya Kiyama wa kuwanusuru na kuwalinda na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

38 Na washirikina juu ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu wameongezea kuikanusha Siku ya Kiyama. Wameapa, ukomo wa nguvu zao za kuapa, na wakakazania kwamba Mwenyezi Mungu hamfufui aliye kufa! Nao ni waongo katika viapo vyao, na Mwenyezi Mungu atawafufua wote! Kwani Yeye amejichukulia ahadi mwenyewe, na Mwenyezi Mungu kabisa hatokwenda kinyume na ahadi yake. Lakini watu wengi miongoni mwa makafiri hawajui hikima ya Mwenyezi Mungu katika kuumba huu ulimwengu, na kwamba Yeye hakuumba kwa mchezo tu, wala wao hawajui hisabu yake na malipo yake.

39 Hakika katika uadilifu wa Mwenyezi Mungu ni kuwa atawafufua wote baada ya kufa kwao ili ipate wadhahirikia hakika ya mambo waliyo khitalifiana. Waumini wapate kujua kuwa wao wako katika Haki, na makafiri wajue kwamba wao walikuwa makosani kwa kumfanyia Mwenyezi Mungu washirika katika Ungu, na pia ni waongo kwa kuapa kwao kwamba Mwenyezi Mungu hamfufui aliye kufa, na ili yote makundi mawili yapate malipo yao kwa kujua na kwa sababu zake.

40. Kauli yetu kwa kitu tunacho kitaka kiwe, ni kukiambia: Kuwa! Basi kinakuwa.⁴⁰
41. Na wale walio hama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu baada ya kudhulumiwa, bila ya shaka tutawaweka duniani kwa wema; na ujira wa Akhera ni mkubwa zaidi; laiti kuwa wanajua!⁴¹
42. Wale wanao subiri na wakamtegemea Mola wao Mlezi.⁴²
43. Nasi hatukuwatuma kabla yako ila watu wanaume tulio wapa Wahyi (Ufunuo). Basi waulizeni wenye ukumbusho kama nyinyi hamjui⁴³
44. Kwa Ishara wazi na Vitabu. Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kufikiri.⁴⁴
45. Je! Wameaminisha wanao fanya vitimbi vya uovu kwamba Mwenyezi Mungu hatawadidimiza katika ardhi, na haitawafika adhabu kutoka wasipo pajua?⁴⁵
46. Au hatawashika katika nyendo zao, na wala hawataponyoka?⁴⁶
47. Au hatawashika kwa kitisho na kuwapunguza kidogo kidogo? Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenye huruma, Mwenye kurehemu.⁴⁷
48. Je! Hawavioni vitu alivyo viumba Mwenyezi Mungu - vivuli vyao vinaelekea kushotoni na kuliani, kumsujudia Mwenyezi Mungu na vikinyenyekea?⁴⁸

40 Na kuwafufua watu Siku ya Kiyama si jambo zito kwetu, hata hao makafiri wakayaona hayawi. Kwani Sisi tutakapo kitu kiwe hatuna haja ya lolote ila ni kusema tu: Kuwa! Na kinakuwa kama tutakavyo.

41 Na Waumini walio yaacha majumba yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na usafi wa imani yao, baada ya kudhulumiwa na washirikina, tutawalipa duniani, kwa ikhlasi yao na kustahamili kwao adhabu, maisha mema yasiyo patikana ila kwa jihadi. Na Siku ya Kiyama ujira wao utakuwa mkubwa zaidi, na neema zao za Peponi ni kubwa zaidi. Lau kuwa wapinzani wao wangeli jua hayo wasingeli wadhulumu na wakazidhulumu nafsi zao

42 Na hao Wahajiri (Walio hama) ndio walio vumilia adhabu walio ipata kwa sababu ya Itikadi yao, na wakamwachia hali yao Mwenyezi Mungu peke yake, bila ya kumbali mwengine. Kwa ajili ya hayo tumewapa bora ya malipo.

43 Na kabla ya kukutuma wewe, ewe Nabii, kwa umma wako, hatukuwatuma kwa kaumu zilizo tangulia ila watu wanaume tulio wafunulia kwa Wahyi yale tunayo yataka wawafikishie. Wala hatukuwatuma Malaika kama watakavyo makafiri wa kaumu yako. Basi, enyi makafiri, waulizeni wenye kuvijua Vitabu vya mbinguni, kama nyinyi hamyajui hayo. Watajua kuwa Mitume wote wa Mwenyezi Mungu hawakuwa ila wanaadamu, wala si Malaika.

44 Na hao Mitume tuliwaunga mkono kwa miujiza na dalili zilizo wazi za kuthibitisha ukweli wao. Na tuliwateremshia Vitabu vya kuwabainishia sharia zao zenye maslaha yao. Na wewe, ewe Nabii, tumekuteremshia Qur'ani uwabainishie watu Itikadi na Hikima ziliomo ndani yake, na uwatake waizingatie, kwa kutaraji kuwa watazingatia, na watawaidhika, na mambo yao yanyooke.

45 Yafaa vipi basi baada ya yote haya kuwa hao washirikina wakaendelea katika inda yao, na wakampangia vitimbi Mtume? Je, kwani wamedanganyika na upole wa Mwenyezi Mungu kwao, hata wakaitakidi kuwa wameaminika na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na ardhi haitowameza kama ilivyo mfanyia Qaarun? Au kuwa adhabu haitowajia kwa ghafla katika kimbunga kama ilivyo wapata kina Thamud nao hawajui inatoka wapi.

46 Au ikawahiliki kati ya nyendo zao katika nchi kwa ajili ya biashara nao wapo mbali na makwao, hata wasiweze kuikwepa adhabu ya Mwenyezi Mungu? Kwani Yeye haemewi na chochote akitakacho.

47 Au akawateremshia adhabu katika nafsi zao na mali yao kidogo kidogo, na hali wao kila wakati wa hiyo adhabu wamo katika khofu na kuingoja iwateremkie. Basi, enyi washirikina! Msiendelee, mkajidanganya kwa kuchelewa adhabu yenu! Upole wake Mwenyezi Mungu ulio enea, na rehema yake iliyo kunjuka, ndio iliyo hukumu asikuleteeni kwa haraka adhabu ya hapa duniani, ili mpate kufikiri na kuzingatia. Kwani Yeye *Subhanahu* ni Mpole na Mwenye kurehemu.

48 Hao makafiri wameghafilika na Ishara za Mwenyezi Mungu zilizo wazunguka. Wala hawatazami wakazingatia vitu alivyo viumba Mwenyezi Mungu vilivyo tulia, na hali vivuli vyake vinakwenda. Mara vinanyookea kulia na mara kushoto, vikifuata mwendo wa jua mchana, na mwendo wa mwezi usiku. Na

49. Na vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi, tangu wanyama mpaka Malaika, vinamsujudia Mwenyezi Mungu, na wala havitakabari.⁴⁹
50. Vinamkhofu Mola wao Mlezi aliye juu yao, na vinafanya vinavyo amrisha.⁵⁰
51. Na Mwenyezi Mungu amesema: Msiwe na miungu wawili! Hakika Yeye ni Mungu Mmoja. Basi niogopeni Mimi tu!⁵¹
52. Na ni vyake Yeye viliomo katika mbingu na ardhi. Na Dini ni yake Yeye daima. Je! Mtamcha mwengine asiye kuwa Mwenyezi Mungu?⁵²
53. Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kisha yakikuguseni madhara mnamyayatikia Yeye.⁵³
54. Na anapo kuondosheeni madhara mara kundi moja miongoni mwenu linamshirikisha Mola wao Mlezi,⁵⁴
55. Wakizikataa neema tulizo wapa. Basi stareheni. Mtakuja jua!⁵⁵
56. Na hao ambao hata hawawajui wanawawekea sehemu ya tunavyo waruzuku. Wallahi! Bila ya shaka mtasailiwa kwa hayo mliyo kuwa mnayazua!⁵⁶
57. Na wanamfanyia Mwenyezi Mungu ati ana mabinti, *Subhanahu*, Aliye takasika! Na wao wenyewe, ati ndio wawe na hayo wanayo yatamani!⁵⁷
58. Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki.⁵⁸
59. Anajificha asionekane na watu kwa ubaya wa aliyo bashiriwa! Je, akae naye juu ya

vyote hivyo vinat'ii amri ya Mwenyezi Mungu, vinafuata hikima ya mipango yake. Na lau washirikina wangeli zingatia haya, wangeli jua kuwa Muumba wake, na Mwenye kuyapanga ni Yeye peke yake anaye stahiki kuabudiwa na kunyenekewa, Muweza wa kuwahiliki akitaka.

49 Ni kwa Mwenyezi Mungu pekee - wala si kwa mwengine - hunyenyekea na kut'ii vyote alivyo viumba mbinguni na viumbe viliomo na vyendavyo katika ardhi. Na mbele yao ni Malaika wanao nyenyekea wala hawatakabari na kumt'ii. (Tazama Maelezo 16:49)

50 Na hali yao ni kuwa daima wamo katika kumkhofu Mola wao Mlezi, Mwenye uwezo na nguvu, na wanafanya anayo waamrisha.

51 Mwenyezi Mungu amesema: Msiabudu wawili, wala msifanye miungu wawili. Kwani kushiriki katika ibada kunapingana na Umoja wa kuumba. Wa kuabudiwa kwa Haki ni Mungu Mmoja tu. Basi niogopeni Mimi wala msimkhofu mwengine.

52 Yeye pekee ndiye mwenye vyote viliomo mbinguni na katika ardhi, kwa kuvumba na kuvimiliki na kumuabudu. Basi ni haki yake Yeye tu pekee kuabudiwa na kuhimidiwa na kunyenekewa, na kutarajiwa rehema yake, na kuogopwa adhabu yake.

53 Na neema yoyote ikikujieni, basi inatoka kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Kisha kikikupatani chochote cha kukudhuruni msiyayatike kwa ukomo wa kelele zenu kwa mwengine yeyote isipo kuwa Yeye.

54 Kisha akiitikia maombi yenu na akakuondoleeni madhara baadhi yenu huisahau Haki ya Mwenyezi Mungu ya Umoja wake na kumsafia ibada Yeye tu, wakamshirikisha Muumba wao na Mlezi wao, na wakawaabudu naye wengine.

55 Hayo hutokea ili mwisho wao huwa kuikanya fadhila yetu kwa yale tuliyo wapa. Basi enyi makafiri! Stareheni na hayo msiyo yatolea Haki ya shukrani. Mtakuja kuujua mwisho wa ukafiri!

56 Na washirikina huyapa masanamu yao, ambayo wanayaita kwa ujinga wao kuwa ni miungu, sehemu ya kujikaribisha kwayo kutokana na zile riziki tulizo wapa Sisi, katika makulima na mifugo na vyenginevyo. Nakuulizeni, kwa Utukufu wangu, enyi washirikina, hayo mliyo khitalifiana kwayo katika uwongo wenu na upotovu mlio uzua. Na Mimi nitakulipeni kwayo.

57 Na hujaalia kumpa Mwenyezi Mungu yale wayachukiayo wao, kwa kudai kuwa Malaika ni watoto wake wa kike, na wao wanawaabudu. Mwenyezi Mungu apishe mbali na hayo! Na wao ati wanajipa wayapendayo nayo ni watoto wanaume.

58 Na akiambiwa mmoja wao kwamba amepata mtoto wa kike, uso wake unasawijika kwa huzuni, naye amejaa hasira na amekasirika.

fedheha hiyo au amfukie udongoni? Tazama uovu wa wanavyo hukumu!⁵⁹

60. Hali ya wasio iamini Akhera ni ovu; na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye sifa tukufu. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.⁶⁰

61. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli wachukulia watu kwa mujibu wa dhulma zao, basi asingeli mwacha hapa hata mnyama mmoja. Lakini anawaakhirisha mpaka muda ulio wekwa. Na unapo fika muda wao hawatakawilia hata saa moja wala hawatatangulia.⁶¹

62. Na wanampa Mwenyezi Mungu wanavyo vichukia wao, na ndimi zao zinasema uwongo kwamba wao watapata mema. Hapana shaka hakika wamewekewa Moto, nao wataachwa humo.⁶²

63. Wallahi! Sisi tulituma Mitume kwa umati zilizo kuwa kabla yako, lakini Shetani aliwapambia vitendo vyao. Kwa hivyo leo yeye ndiye rafiki yao; nao watapata adhabu chungu.⁶³

64. Na hatukukuteremshia Kitabu isipo kuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitalifiana, na kiwe Uwongofu na Rehema kwa watu wanao amini.⁶⁴

65. Na Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mbinguni na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Kwa hakika katika hayo imo Ishara kwa watu wanao sikia.⁶⁵

66. Na hakika katika nyama hoa nyinyi mna mazingatio. Tunakunywesheni katika vile viliomo matumboni mwao, vikatoka baina ya mavi na damu, maziwa safi mazuri kwa wanywao.⁶⁶

59 Anajaribu kujificha watu wasiione huzuni ya machungu yaliyo mpata kwa kupewa khabari ya binti aliye zaliwa. Anapatapa: amwache hai juu ya fedheha anayo iona, kama anavyo jigamba? Au amzike katika udongo naye yuhai mpaka afe? Ewe msikilizaji! Zingatia uwovu wa vitendo vya watu hawa! Na uovu gani wa kumhukumia Mwenyezi Mungu mabinti ambao wao wanawachukia!

60 Ni hali mbaya ya wasio amini Akhera na yote yaliyoko huko ya thawabu na adhabu, nayo ni ile haja ya kutaka watoto wa kiume na kuchukia watoto wa kike. Na Mwenyezi Mungu ana sifa tukufu. Yeye ni Mkwasi, hahitajii kitu, wala hana haja ya mtoto. Naye ni Mwenye kushinda, Mwenye nguvu, wala hana haja ya msaidizi.

61 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli fanya haraka kuwadhibu watu kwa dhulma zao wanazo zifanya, basi asingeli mwacha hata mnyama mmoja juu ya ardhi. Lakini Yeye kwa upole wake na hikima yake anawaakhirisha madhaalimu mpaka wakati aliyo uweka, nao ndio wakati utapo kwisha muda wao. Ukija wakati huo hawato taakhari hata kidogo, wala hawato tangulia.

62 Na washirikina wanamnasibisha Mwenyezi Mungu mabinti na ushirika mambo ambayo wao wanayachukia. Na ndimi zao zinatamka uwongo wanapo dai ya kwamba, kama walivyo kuwa na utajiri na utawala duniani, basi kadhaalika Akhera nao watapata malipo mema kwa Mwenyezi Mungu watapo fufuliwa; nayo ni Pepo! Hapana shaka hao watatiwa Motoni, nao watasukumwa huko kabla ya wengineo.

63 Ewe Nabii! Jua kwa yakini kwamba Sisi tuliwatuma Mitume kabla yako kwa kaumu nyingi kama tulivyo kutuma wewe kwa watu wote. Lakini Shetani aliwapambia ukafiri, na ushirikina, na maasi. Basi wakawakanya Mitume wao, na wakawaasi, na wakamsadiki Shetani na wakamt'ii yeye. Basi yeye amekuwa ndiye mwenye kuyatawala mambo yao katika dunia, akiwapambia mambo ya kuwadhuru. Na Akhera watapata adhabu yenye machungu makali.

64 Na hatukukuteremshia wewe hii Qur'ani isipo kuwa upate kuwabainishia watu haki katika yale waliokhitalifiana kwayo katika dini, na ili ipate kuwa ni uwongofu ulio timia na rehema ilio enea kwa kaumu yenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Kitabu alichokuteremsha.

65 Na Mwenyezi Mungu ameteremsha kutoka mbinguni maji yanayo bebwa na mawingu, akaifanya ardhi ikamea na ikawa na uhai, baada ya kuwa kabla yake kavu haina uhai. Hakika katika hayo pana dalili wazi ya kuwepo Mwenye kudabiri Mwenye hikima. (*Tazama Maelezo 16:65*)

66 Na enyi watu! Hakika katika nyama hoa, yaani mifugo, ngamia, ng'ombe, na kondoo na mbuzi, mna mawaidha yanayo faa kuzingatiwa na kufuatwa uwongofu wake wa kumtoa mtu ujingani akaingia

67. Na kutokana na matunda ya mitende na mizabibu mnatengeneza ulevi na riziki nzuri. Hakika katika hayo ipo Ishara kwa wanao tumia akili.⁶⁷
68. Na Mola wako Mlezi amemfunulia nyuki: Jitengenezee majumba yako katika milima, na katika miti, na katika wanayo jenga watu.⁶⁸
69. Kisha kula katika kila matunda, na upite katika njia za Mola wako Mlezi zilizo fanywa nyepesi kuzipita. Na kutoka matumbo yao kinatoka kinywaji chenye rangi mbali mbali; ndani yake kina matibabu kwa wanaadamu. Hakika katika haya ipo Ishara kwa watu wanao fikiri.⁶⁹
70. Na Mwenyezi Mungu amekuumbeni; kisha anakufisheni. Na miongoni mwenu wapo wanao rudishwa kwenye umri mbaya kabisa, hata akawa asijue kitu baada ya ujuzi alio kuwa nao. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi na Mweza.⁷⁰
71. Na Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu kuliko wengine katika riziki. Na wale walio fadhilishwa hawarudishi riziki zao kwa wale ilio wamiliki mikono yao ya kulia ili wawe sawa katika riziki hiyo. Basi je, wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu?⁷¹
72. Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni wake katika jinsi yenu, na akakujaalieni kutoka kwa wake zenu wana na wajukuu, na akakuruzukuni vitu vizuri vizuri. Basi je, wanaamini upotovu na wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu?⁷²

kumjua Mwenye kuumba, Aliye anzisha kila kitu, Mwenye hikima. Na Sisi tunakunyesheni kutokana na baadhi ya viliomo matumboni mwa hao wanyama vilio zidi katika chakula na damu maziwa safi, matamu, mepesi kuyapata kwa wanao kunywa. (*Tazama Maelezo 16:66*)

67 Na kutokana na matunda ya mitende na mizabibu tuliyo kuneemesheni kwayo na tukakuwezesheni kuitumia, mnakamua maji yake yakatoka ulevi usio kuwa mzuri, na chakula kilicho kuwa kizuri. Hakika katika haya pana alama yenye kuonyesha uwezo na rehema kwa watu wanao nafiika kwa akili zao. (Kitu kile kile kina faida kikitumiwa kwa sharia za Mwenyezi Mungu za maumbile, na kile kile kikawa na madhara kikitumiwa kinyume na hizo sharia.)

68 Ewe Nabii! Zingatia jinsi Mwenyezi Mungu alivyo mfahamisha nyuki, kama kwamba amemfunulia kwa Wahyi, akamwonyesha sababu za uhai wake, na njia za maisha yake. Akamfunza ajenge masega yake katika mapango, na katika uwazi wa miti, na kwenye maburuji ya majumba na mizabibu.

69 Kisha *Subhanahu* akamhidi Nyuki ale matunda ya miti na mimea mbali mbali, na akamsahilishia afuate njia alizo mtegemeza Mola wake Mlezi, na akatoa kutokana na matumbo yake kinywaji, nacho ni asali, chenye rangi mbali mbali. Na hiyo asali imekuwa ni dawa ya kuwaponyesha watu. Hakika katika hayo pana ufundi wa ajabu wa kuonyesha nguvu, na kuwepo Mwenye kuumba, na Mwenye kuweza, Mwenye hikima. Wenye kutumia akili zao wananufaika kwa mazingatio hayo, na watapata furaha ya daima. (*Tazama Maelezo 16:69*)

70 Mwenyezi Mungu amekuumbeni, na amekujaalieni kila mtu na ajali yake. Kati yenu wapo wanao kufa mapema, na wengine wanao fikia ukongwe wakarejea katika hali ya udhaifu. Wakawa wanadhoojika kidogo kidogo, zikipungua nguvu zao za mwili, na mifupa na viungo na mishipa. Mwisho wao wakawa hawajiwezi kujifanyia lolote liwapasalo! Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa siri za kuumba kwake, ni Muweza wa kutimiza alitakalo.

71 Na Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu kwa riziki kuliko wengineo. Amemruzuku bwana mwenye kumiliki kuliko mtumwa mamluki. Wala walio ruzukiwa kingi hawawapi watumwa wao hata nusu ya riziki yao, ili wapate kuwa wote na riziki sawa! Basi ikiwa hawa makafiri hawakubali watumwa wao washirikiane nao katika riziki iliyo toka kwa Mwenyezi Mungu, nao wote ni wanaadamu kama wao, basi vipi wao wanataka kumshirikisha Mwenyezi Mungu na viumbe vyake katika mambo yasio kuwa laiki naye *Subhanahu wa Taa'la*, nako ni kustahiki kuabudiwa? Basi je, macho ya hao washirikina yataendelea kufumbika baada ya yote haya, wakabaki wakipinga neema za Mwenyezi Mungu juu yao kwa kumshirikisha Yeye na wengineo?

72 Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni wake wa jinsi yenu mtulie nao. Tena amekupeni, kutoka kwa wake zenu, wana na wajukuu, na akakuruzukuni vitu vya kufurahisha nafsi zenu alivyo kuhalalishieni.

73. Na badala ya Mwenyezi Mungu wanawaabudu wasio wamilikia riziki kutoka mbinguni wala kwenye ardhi, wala hawawezi kitu.⁷³
74. Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano. Hakika Mwenyezi Mungu anajua, na nyinyi hamjui.⁷⁴
75. Mwenyezi Mungu anapiga mfano wa mtumwa aliye milikiwa, asiye weza kitu, na mwingine tuliye mruzuku riziki njema inayo toka kwetu, naye akawa anatoa katika riziki hiyo kwa siri na dhaahiri. Je, hao watakuwa sawa? Alhamdu Lillahi! Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui.⁷⁵
76. Na Mwenyezi Mungu anapiga mfano wa watu wawili. Mmoja wao ni bubu, hawezi chochote, naye ni mzigo kwa bwana wake. Popote anapo muelekeza haleti kheri. Je! Huyu anaweza kuwa sawa na yule anaye amrisha uadilifu, naye yuko juu ya Njia Iliyo Nyooka?⁷⁶
77. Na siri zote za katika mbingu na ardhi ziko kwa Mwenyezi Mungu. Wala halikuwa jambo la Saa (ya Kiyama) ila kama kupepesa kwa jicho, au akali ya hivyo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.⁷⁷
78. Na Mwenyezi Mungu amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa

Je, baada ya haya ndio baadhi ya watu humshirikisha Mwenyezi Mungu, na wakaamini upotovu, na wakazipinga neema za Mwenyezi Mungu zinazo onekana, ambazo zinastahiki shukrani kutoka kwao, na kumsafia ibada Mwenyezi Mungu? (*Tazama Maelezo 16:72*)

73 Na wakawa badala ya Mwenyezi Mungu wakaabudu masanamu ambayo hayawezi kuwapa riziki yoyote hata chembe, sawa sawa ikiwa riziki hiyo inatoka mbinguni kama maji, au kutokana na ardhi kama matunda ya miti na mimea. Na miungu hiyo haiwezi kufanya lolote kama hayo, wala duni ya hayo!

74 Na iliyo kuthibitikieni kuwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu hakufaeni kitu, basi msiseme kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ana yeyote wa kumshabihi, ikawa kisingizio cha kuwaabudu hao kwa vipimo vipotovu, na kushabihisha kusio kweli kwa ajili ya kuwaabudu hao pamoja naye! Hakika Mwenyezi Mungu anajua upotovu wa mnayo yatenda, naye atakulipeni kwayo na hali nyinyi mmo katika mghafala hamjui ubaya wa mwisho wenu

75 Mwenyezi Mungu amepiga mfano kufahamisha ufisadi walio nao washirikina. Mtumwa aliye milikiwa kama mtumwa mamluki, hanalo aliwezaloo kulitenda; na muungwana anaye ruzukiwa na Mwenyezi Mungu riziki ya halali, naye anatoa katika hiyo riziki kwa siri na dhaahiri! Je, ni sawa watumwa wasio weza kitu, na waungwana wenye nacho na wanatumia walicho nacho? Hakika Mwenyezi Mungu anamiliki kila kitu, na anafanya katika ufalme wake kama apendavyo. Na asiye kuwa Yeye hamiliki chochote. Basi huyo hastahiki kuabudiwa na kuhimidiwa. Sifa zote ni haki ya Mwenyezi Mungu peke yake. Yeye ndiye Mwenye Utukufu peke yake, kwani kila kheri inatoka kwake, na kila zuri linarejea kwake. Wala hawatendi hao wanayo yatenda kwa kujua, bali wanatenda kwa kuwafuata wakubwa zao. Bali wengi wao hawajui, na wanaziambatisha neema za Mwenyezi Mungu kwa wengineo, na wanawaabudu hao badala yake!

76 Mwenyezi Mungu amekupigieni mfano mwengine, wa watu wawili. Mmoja wao kiziwi-bubu; hafahamu wala hafahamiki, mzigo kwa aliye mlazimu kumtazama. Bwana wake akimuelekeza kokote harejei na faida yoyote. Basi, je, mtu huyu atakuwa sawa na mtu mwinginewe aliye fasihi wa kusema, anasikia vyema, anaamrisha haki na uadilifu, naye mwenyewe ameshika Njia iliyo kaa sawa, isiyo kwenda upogo? Huyu kiziwi asiye sikia wala kusema wala hafahamu wala hafahamiki, ndio mfano wa masanamu wanayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Kwani hayo hayasikii wala hayasemi wala hayafai kitu. Hayawezi hayo kulingana na Mwenye kusikia, Mwenye kujua, Mwenye kuwaita watu wende kwenye kheri na haki, na kwenye Njia Iliyo Nyooka.

77 Na ni ya Mwenyezi Mungu tu peke yake yote wasiyo yajua waja katika mbingu na katika ardhi. Wala jambo la kuja Siku ya Kiyama, na kufufuliwa watu, haraka yake na upesi wake kwa Mwenyezi Mungu, si chochote ila ni kama kufumba na kufumbua jicho! Bali ni duni kuliko hivyo, jinsi ya upesi wake. Hakika uwezo wa Mwenyezi Mungu ni mkubwa mno, Yeye haemewi na kitu.

hamjui kitu, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru.⁷⁸

79. Je! Hawawaoni ndege walivyo wat'iifu katika anga la mbingu? Hapana mwenye kuwashika isipo kuwa Mwenyezi Mungu. Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanao amini.⁷⁹

80. Na Mwenyezi Mungu amekujaalieni majumba yenu yawe ni maskani yenu, na amekujaalieni kutokana na ngozi za wanyama nyumba mnazo ziona nyepesi wakati wa safari zenu na wakati wa kutua kwenu. Na kutokana na sufi zao na manyoya yao na nywele zao mnafanya matandiko na mapambo ya kutumia kwa muda.⁸⁰

81. Na Mwenyezi Mungu amekufanyieni vivuli katika vitu alivyo viumba, na amekufanyieni maskani milimani, na amekufanyieni nguo za kukingeni na joto, na nguo za kukingeni katika vita vyenu. Ndio hivyo anakutumizieni neema zake ili mpate kut'ii.⁸¹

82. Basi wakikengeuka lilio juu yako wewe ni kufikisha ujumbe wazi wazi.⁸²

83. Wanazijua neema za Mwenyezi Mungu, kisha wanazikanusha; na wengi wao ni makafiri.⁸³

84. Na siku tutakapo wainua kutokana na kila umma shahidi, kisha hawataruhisiwa walio kufuru wala hawataachiliwa kutaka radhi.⁸⁴

85. Na walio dhulumu watakapo iona adhabu hawatapunguziwa hiyo adhabu, wala

78 Na Mwenyezi Mungu amekutoeni kutokana na matumbo ya mama zenu hali hamjui chochote katika yaliyo kuzungukeni. Na akakupeni kusikia na kuona na nyoyo, kuwa ndio silaha za kujifunzia na kufahamu, ili mpate kumuamini kwa njia ya ilimu, na mumshukuru kwa alivyo kufadhilini. (*Tazama Maelezo 16:78*)

79 Je! Hao washirikina hawawaangalii ndege walio jaaliwa waweze kuruka hewani juu, kwa kupewa na Mwenyezi Mungu mbawa kubwa kuliko miili yao, wakiikunjua na kuikunja. Na Mwenyezi Mungu akaidhalilisha hewa kuwabeba hao ndege. Hapana anaye washika huko angani ila Mwenyezi Mungu kwa nidhamu aliyoteengeza Yeye Mwenyewe! Hakika katika kuwatazama hao ndege, na kuzingatia hikima ya Mwenyezi Mungu katika kuwaumba, ni ishara kubwa ya kuwanafiisha walio kuwa tayari kuamini. (*Tazama Maelezo 16:79*)

80 Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* ndiye aliyekujaalieni mkaweza kusimamisha nyumba zenu ili ziwewe maskani yenu. Na akakujaalieni kutokana na ngozi za ngamia, na ng'ombe, na kondoo na wanyama wengineo mkafanya mahema ambayo ni kama nyumba za kukalia, na mkihama nayo mnapo safari na mnapo tua. Na kutokana na sufi zao, na nywele zao, na manyoya yao, mkafanya matandiko ya kutumia hapana duniani mpaka itakapo fika ajali yenu ya kuondoka.

81 Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni miti na vitu vyenginevyo vya kukupeni vivuli kukulindeni na taabu ya joto, na amekufanyieni mapango milimani, nanyi mkafanya humo maskani kama nyumba. Pia amekuumbieni nguo za sufi na pamba na kitani na vyenginevyo, ili kukuhifadhini na joto la jua, na nguo za chuma za kukulindeni katika vita na adui zenu. Kama alivyo kujaalieni hayo, basi kadhaalika amekutumizieni neema zake kwa kukupeni Dini iliyo simama sawa, ili mpate kuifuata amri yake, na mumsafie ibada Yeye tu si na mwengineuwe.

82 Wakikupuza, ewe Nabii, hao unao waita wafuate Uislamu, basi wewe huna jukumu kwa mapuuzi yao. Haikulazimu wewe ila kufikisha ujumbe kwa uwazi, na hayo umekwisha fanya.

83 Kupuuza kwao hao makafiri si kwa kuwa hawajui kwamba Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ndiye chanzo cha kila neema zote wanazo zipata, lakini wao hutenda vitendo vya wanao kanya neema, kwa vile hawamshukuru Mola Mlezi kwazo. Na wengi wao wamekazania kuwafuata baba zao katika kumkataa Mwenyezi Mungu, mpaka wakawa wengi wao ndio wapinzani.

84 Ewe Nabii! Mhadharishe kila anaye mkataa Mola wake Mlezi kwa yatakayo tokea Siku tutakapo muinua kutokana na kila umma shahidi wa kuwashuhudia kwa walivyo mpokea Mtume wa Mola wao Mlezi. Na pindi akitaka kafiri kutoa udhuru, hatapewa ruhusa ya kutaka kutoa udhuru. Wala hatapatikana mwombezi wa kumtengenezea maombezi, kwa kutakiwa warejee waache sababu za Mwenyezi Mungu kuwakasirikia. Kwani Akhera sio pahala pa kutubia.

hawatapewa muhula.⁸⁵

86. Na walio shirikisha watakapo waona hao walio washirikisha na Mwenyezi Mungu, watasema: Mola wetu Mlezi! Hawa ndio washirikishwa wetu ambao tulikuwa tukiwaabudu badala yako. Ndipo wale watakapo watupia kauli: Hakika nyinyi ni waongo!⁸⁶

87. Na siku hiyo watasalimu amri mbele ya Mwenyezi Mungu, na yatapotea waliyo kuwa wakiyazua.⁸⁷

88. Wale walio kufuru na kuzuilia Njia ya Mwenyezi Mungu tutawazidishia adhabu juu ya adhabu, kwa walivyo kuwa wakifisidi.⁸⁸

89. Na (waonye) siku tutakapo wainua mashahidi katika kila umma wakiwashuhudia kwa yanayo tokana na wao, na tutakuleta wewe uwe shahidi juu ya hao. Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu.⁸⁹

90. Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka.⁹⁰

91. Na timizeni ahadi ya Mwenyezi Mungu mnapo ahidi, wala msivunje viapo baada ya kuvithibitisha, ilihali mmekwisha mfanya Mwenyezi Mungu ndiye mdhamini wenu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua myatendayo.⁹¹

85 Na wale walio jidhullumu nafsi zao kwa kukufuru watakapo iona Jahannamu, na wakataka wapunguziwe adhabu, hawato jibiwa, wala hawato akhishwa kuingia Jahannamu hata dakika moja.

86 Na walio wafanya miungu yao washirika wa Mwenyezi Mungu na wakawaabudu watapo sema: Ewe Mola Mlezi wetu! Hawa ndio washirikishwa wetu tulio tukiwaabudu kwa makosa. Basi tupunguzie adhabu kwa kuwapa wao baadhi ya adhabu! Washirikishwa wao watajibu: Ama hakika nyinyi washirikina waongo kwa kudai kwenu kuwa sisi ni washirika wa Mwenyezi Mungu, na kwamba nyinyi mkituabudu! La kweli ni kuwa mkiabudu matamano yenu tu, wala sisi hatukuwa washirika kama mlivyo dai. (Nabii Isa a.s. amesema: "Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe, ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu." - Injili ya Mathayo 7.21-27).

87 Hapo tena wale washirikina walio mshirikisha Mwenyezi Mungu watasalimu amri, waikubali hukumu yake, na yawaondokee yale mawazo yao kwamba walio kuwa wakiwaabudu yatakuja waombea na kuwakinga na adhabu!

88 Walio kufuru na wakawazua wengine kufuata Njia ya Mwenyezi Mungu, nayo ndiyo Njia ya kheri na haki, tutawazidishia adhabu juu ya adhabu wanayo stahiki kwa ukafiri wao, kwa walivyo kusudia kuwafisidi na kuwapotosha waja wa Mwenyezi Mungu!

89 Ewe Nabii! Wahadharishe makafiri katika kaumu yako kwa yatakayo wapata Siku tutapo watolea kila umma shahidi wa kuwashuhudia, naye ndiye Nabii wao, ambaye atakuwa ni mmoja wao, ili wawe hawana kisingizio. Na wewe, ewe Nabii, tutakuleta uwashuhudie hao walio kukadhibisha. Na tangu hivi sasa yawapasa wazingatie! Sisi tumekuteremshia wewe Qur'ani, ambayo ndani yake kila kitu kimebainishwa kwa haki. Na ndani yake umo uwongofu, na rehema, na bishara ya Pepo kwa wenye kuifuata na kuiamini.

90 Mwenyezi Mungu anawaamrisha waja wake uadilifu wa maneno na vitendo, na katika kila jambo wakusodie lilio bora, na walifadhilisha kuliko jengino. Kama anavyo amrisha kuwapa jamaa zenu wanacho hitajia, ili kuzidi kutia nguvu makhusiano ya mapenzi kati ya ukoo. Na Mwenyezi Mungu anakataza kutenda kila la makosa, na khasa madhambi yaliyo pita mpaka kwa ubaya, na kila kisicho pendeza katika sharia na akili nzuri. Hali kadhaalika anakataza kumfanyia uadui mtu. Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika anakukumbusheni haya, na anakuelekezeni kwenye mambo mema, mpate kukumbuka fadhila zake kwa maelekezo yake mema, basi ndio mfanye anavyo kwambieni.

91 Na timizeni ahadi mlizo jitolea nafsi zenu kwa kumshuhudisha Mwenyezi kuwa mtazitekeleza, maadamu ahadi hizo ni kwa mujibu wa sharia ya Mwenyezi Mungu. Wala msivunje viapo vyenu kwa kutotimiza baada ya kuvitilia nguvu kwa kumtaja Mwenyezi Mungu, na kuazimia kikweli kutimiza. Nanyi mlipo toa ahadi mlitia maanani kuwa Mwenyezi Mungu ndiye dhamini wenu kwamba mtatekeleza, na kwamba Mwenyezi Mungu anakuangalieni na kukuoneni. Basi shikamaneni na ahadi zenu na viapo

92. Wala msiwe kama mwanamke anaye uzongoa uzi wake baada ya kwisha usokota ukawa mgumu. Mnavifanya viapo vyenu kuwa ni njia ya kudanganyana baina yenu kwa kuwa ati taifa moja lina nguvu zaidi kuliko jengine? Hakika Mwenyezi Mungu anakujaribuni kwa njia hiyo. Na bila ya shaka atakubainishieni Siku ya Kiyama mliyo kuwa mkikhitalifiana.⁹²

93. Na Mwenyezi Mungu angeli taka, kwa yakini angeli kufanyeni umma mmoja. Lakini anamwachia kupotea anaye mtaka, na anamwongoa amtakaye. Na hakika mtaulizwa kwa yale mliyo kuwa mkiyafanya.⁹³

94. Wala msifanye viapo vyenu ni njia ya kudanganyana baina yenu. Usije mguu ukateleza badala ya kuthibiti, na mkaonja maovu kwa sababu ya kule kuzuilia Njia ya Mwenyezi Mungu, na mkapata adhabu kubwa.⁹⁴

95. Wala msinunue ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa thamani ndogo. Hakika kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ndicho bora kwenu, ikiwa mnajua.⁹⁵

96. Mlivo navyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ndivyo vitakavyo bakia. Na kwa yakini Sisi tutawapa walio subiri ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.⁹⁶

97. Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa

vyenu, kwani Mwenyezi Mungu *Subhanahu* anakujueni yupi katika nyinyi anaye timiza na anaye kwenda kinyume, yupi anaye tekeleza na yupi anaye vunja. Basi atakulipeni kwa mnayo yafanya.

92 Wala msiwe katika kwenda kinyume na viapo vyenu baada ya kuvithibitisha mfano wa mwanamke mwendawazimu anaye sokoto sufi, ikisha kuwa nyuzi akazifumua tena. Mkafanya viapo vyenu kuwa ni njia ya kudanganya na kukhadaa watu, na huku mkijitafutia udhuru kwa kuwa ama nyinyi ni wengi zaidi au mna nguvu zaidi kuliko wao, au mnakusudia kuwaunga mkonu maadui wenye nguvu zaidi kuliko wao, au kwa kuwa mnataraji kuzidi nguvu kwa khiana! Na hakika Mwenyezi Mungu anakufanyieni mtihani. Mkikhiari kutimiza ahadi mtapata mavuno ya duniani na Akhera. Mkielekea khiana, basi ni khasara yenu. Na hakika Siku ya Kiyama atakubainishieni ukweli wa khitalafu zenu za duniani, na atakulipeni kwa mujibu wa vitendo vyenu. (*Tazama* Maelezo 16:92)

93 Mwenyezi Mungu ange taka angeli kufanyeni nyote umma wa namna moja kwa jinsi, na rangi, na imani, bila ya khitalafu. Na hayo ni kwa kukupeni umbo jengine, mkawa kama Malaika wasio na uwezo wa kukhiari watakalo. Lakini ametaka muwe jinsi na rangi mbali mbali, na akakupeni uwezo wa kukhiari wenyewe. Mwenye kukhiari matamano ya dunia kuliko kumridhi Mwenyezi Mungu, anaachwa kwa ayatakayo. Na mwenye kutaka kumridhi Mwenyezi Mungu kwa vitendo vyema, anasahilishiwa kwa anayo yataka. Na kuweni na yakini kuwa nyote nyinyi mtakuja ulizwa Siku ya Kiyama juu ya mliyo yatenda duniani, na mtalipwa kwa vitendo vyenu.

94 Wala msishike njia ya khiana, mkafanya viapo ndio njia ya udanganyifu na khadaa. Kwa hivyo nyayo zenu zitateleza mlikosee lengo lilio sawa, na kwa hivyo ikapelekea mkaiwacha Njia ya Mwenyezi Mungu ya kutimiza ahadi, na mkawa ni mfano muovu wa khiana, na watu wakaja waona kuwa Waislamu ni watu wabaya, na wakautupilia mbali Uislamu wenyewe. Na uovu ukateremka duniani kwa sababu yenu kwa kuto kuaminini kwa vile mnavyo kwenda kinyume na njia ya haki, nanyi ikakuteremkieni adhabu kali yenye kutia machungu.

95 Wala msibadilisha ahadi ya kweli kweli kwa kutaka pato la dunia, na hilo ni duni na lingali onekana kubwa. Maana yaliopo kwa Mwenyezi Mungu, malipo ya wanao hifadhi ahadi zao duniani, na malipo ya Akhera ya milele, ni bora kwenu kuliko yote yanayo kudanganyeni kwa kuvunja ahadi. Basi zingatieni na mfahamu, ikiwa nyinyi ni watu wa ilimu na utambuzi baina ya jema na lisio kuwa jema. Wala msitende ila lilio na maslahi kwenu duniani na Akhera.

96 Kwani neema mlizo nazo zina mwisho hata zingeli kaa muda mrefu. Na neema zilioko kwa Mwenyezi Mungu Akhera ni za milele wala hazishi. Na Sisi tutawalipa wenye kuvumilia mashaka ya taabu kwa ajili ya tuliyo waahidi, nayo ni kupata bora ya malipo marudufu kwa vitendo vyao, waneemeke kwayo daima milele Akhera.

wakiyatenda.⁹⁷

98. Na ukisoma Qur'ani mwombe Mwenyezi Mungu akulinde na Shetani maluuni.⁹⁸

99. Hakika yeye hana madaraka juu ya walio amini na wakamtegemea Mola wao Mlezi.⁹⁹

100. Hakika madaraka yake ni juu ya wanao mfanya rafiki yao, na wale wanao fanya ushirika naye.¹⁰⁰

101. Na tunapo badilisha Ishara pahala pa Ishara nyengine, na Mwenyezi Mungu anajua anayo teremsha, wao husema: Wewe ni mzushi. Bali wengi wao hawajui kitu.¹⁰¹

102. Sema: Ameiteremsha hii Roho takatifu kutokana na Mola wako Mlezi kwa haki, ili awathibitisha wale walio amini, na kuwa ni uwongofu, na ni bishara kwa Waislamu.¹⁰²

103. Na Sisi hakika tunajua kwamba wanasema: Yuko mtu anaye mfundisha. Lugha ya huyo wanaye muelekezea ni ya kigeni, na hii ni lugha ya Kiarabu mbayana.¹⁰³

104. Hakika wasio ziamini Ishara za Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu hawaongoi, nao watapata adhabu chungu.¹⁰⁴

97 Hakika mwenye kutenda mema duniani, sawa sawa akiwa mwanamume au mwanamke, akajiingiza katika huo wema kwa nguvu za imani, kwa kila linalo wajibika kwa kuliadini, basi Sisi hatuna budi kumfanya aishi maisha mazuri yasiyo kuwa na machungu, yenye ndani yake ukinaifu na kuridhika na kuvumilia masaibu ya dunia, na shukrani kwa neema anazo zipata kwa Mwenyezi Mungu. Na Akhera hapana budi ya kuwa tutawalipa watu wa namna hii bora ya malipo kwa kuzidi marudufu kwa vitendo vyao vya duniani.

98 Kinacho linda nafsi isighurike na pumbao ni Qur'ani. Ewe Muumini! Ukitaka kuishi maisha ya mbali na kuchezewa na Shetani, na upate wema wa kote kuwili, duniani na Akhera, basi Mimi nakuongoza kwenye jambo litakalo kusaidia kwa hayo. Jambo lenyewe ni kuisoma Qur'ani. Na unapo taka kusoma Qur'ani, anzia kwa kumuomba Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi akuepushe na wasiwasi wa Shetani, aliye fukuzwa kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu, na anaona uzuri kuwaghuri watu awaingize katika kumuasi Mwenyezi Mungu.

99 Ukifanya haya kwa kumsafia niya Mwenyezi Mungu, basi atakulinda na Shetani, na atakuondolea wasiwasi. Kwani Shetani hana athari kwa walio jaa Imani ya Mwenyezi Mungu, na wakamtaka msaada na kumtegemea Yeye peke yake.

100 Bali taathira yake Shetani na khatari yake ni juu ya wale ambao nyoyo zao hazina mfungamano wala mapenzi na Mwenyezi Mungu. Basi hao hawana la kuwalinda na athari za Shetani. Watamfuata huyo kama rafiki anavyo mfuata rafiki yake, mpaka watumbukie katika kumshirikisha Mwenyezi Mungu katika kumuabudu pamoja na miungu mingine isiyoweza kuleta madhara wala manufaa.

101 Na tukikuletea muujiza badala ya muujiza ulio sawa na tulio waletea Manabii walio tangulia, na tukakuletea wewe hii Qur'ani kuwa ni muujiza wenyewe, wanakusingizia kuwa umeizua tu hii, na kwamba unamzulia Mwenyezi Mungu uwongo! Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mjuzi kwa ujuzi usio pikuliwa kujua miujiza anayo wateremshia Manabii wake. Lakini wengi wao watu hawa si watu wa ilimu wa kujua lilio kweli.

102 Ewe Nabii! Waambie kuwabainishia muujiza wako: Hakika hii Qur'ani kaniteremshia mimi Jibril, Roho safi, kutokana kwa Mola wangu Mlezi, kwa kufuatana na kukusanya Haki, ili kwayo azitie imara nyoyo za Waumini, na ili iwe ni Uwongofu kwa watu wote waongokewe, na iwape bishara njema ya neema Waislamu wote.

103 Hakika Sisi tunajua wayasemayo makafiri wa Makka, nayo: Hamfundishi Muhammad hii Qur'ani ila mtu tunaye mjua, naye ni kijana wa Kirumi. Wala hamteremshii Malaika kutoka kwa Mwenyezi Mungu kama asemavyo! Na kauli yao hii ni ya uwongo. Kwani huyo kijana wanaye sema kuwa anakufundisha wewe ni mgeni, hajui Kiarabu vizuri. Na Qur'ani ni lugha ya Kiarabu kilicho wazi cha ufasihi, hata imekuwa nyinyi wabishi mmeshindwa kuleta mfano wake. Basi hizo tuhuma zenu zina maana gani?

104 Hakika hao wasio zikubali Ishara za Mwenyezi Mungu ambazo wameshindwa kuleta mfano wake, na wakashikilia kuzikataa juu ya kuemewa kwao, Mwenyezi Mungu hawaongoi. Nao Akhera watapata adhabu kali kwa sababu ya ukafiri wao na inadi yao!

- 105.** Wanao zua uwongo ni wale tu wasio ziamini Ishara za Mwenyezi Mungu. Na hao ndio waongo.¹⁰⁵
- 106.** Anaye mkataa Mwenyezi Mungu baada ya kuamini kwake - isipo kuwa aliye lazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetua juu ya Imani, lakini aliye kifungulia kifua chake kukataa - basi hao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ipo juu yao, na wao watapata adhabu kubwa.¹⁰⁶
- 107.** Hayo ni kwa sababu wameyapenda zaidi maisha ya duniani kuliko ya Akhera, na kwa sababu Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri.¹⁰⁷
- 108.** Hao ndio Mwenyezi Mungu ameziziba nyoyo zao na masikio yao na macho yao. Na hao ndio walio ghafilika.¹⁰⁸
- 109.** Hapana shaka ya kwamba hao ndio wenye kukhasiri Akhera.¹⁰⁹
- 110.** Kisha hakika Mola wako Mlezi, kwa wale walio hama makwao baada ya kuteswa, kisha wakapigania Dini na wakasubiri, bila ya shaka Mola wako Mlezi baada ya hayo ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.¹¹⁰
- 111.** Siku ambayo kila nafsi itakuja jitetea, na kila nafsi italipwa sawa sawa na a'mali ilizo zifanya, nao hawatadhulumiwa.¹¹¹
- 112.** Na Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mji ulio kuwa na amani na utulivu, riziki yake ikiufikia kwa nafasi kutoka kila mahali. Lakini ukazikufuru neema za Mwenyezi Mungu; kwa hivyo Mwenyezi Mungu akauvika vazi la njaa na khofu kwa sababu ya yale waliyo kuwa wakiyafanya.¹¹²

105 Hakika wanao jasirisha kumzulia Mwenyezi Mungu uwongo ni wale wasio ziamini Ishara za Mwenyezi Mungu, na hao peke yao ndio walio fikilia ukomo wa uwongo. Na wewe, Nabii, si katika watu hao hata wa kutuhumie hivyo.

106 Hao wanao tamka ukafiri baada ya kuamini watapata ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Isipo kuwa aliye lazimishwa kutamka maneno ya ukafiri na hali moyo wake umesimama imara katika Imani. Huyu atavuka, haitompata ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Ama ambao nyoyo zao zinafurahia ukafiri, na ndimi zao zinakubaliana na yaliyo nyoyoni mwao, hao watapata ghadhabu kali kwa Mwenyezi Mungu ambaye amewaandalia adhabu kubwa katika Akhera.

107 Na hiyo ghadhabu na adhabu waliyo stahiki kuipata, ni kwa sababu ya kupenda kwao mno neema za duniani na starehe zake za kupita njia, hata zikawaweka mbali na Haki, na zikawatia upofu wasiione kheri. Basi Mwenyezi Mungu akawaachilia mbali na huo ukafiri wanao upenda. Huo ndio mwendo wake anavyo watendea viumbe vyake, huwaacha kama hawa, na huwaacha asiwahidi kwa sababu ya ufisadi wao wenyewe, na kukakamia katika upotovu.

108 Hao ndio Mwenyezi Mungu amewapiga muhuri wa mghafala katika nyoyo zao, hata zikawa haziikubali Haki, na katika masikio yao wakawa hawasikii kwa sikio la fahamu na mazingatio wakawa kama viziwi, na katika macho yao hata wakawa hawaoni ishara na dalili zilizo mbele yao. Hao ndio walio zama katika kughafilika na Haki. Hao hawana kheri mpaka uondoke mghafala katika akili zao.

109 Hao hapana shaka yoyote ndio peke yao watakao khasiri kila kheri katika Akhera.

110 Tena, ewe Nabii! Jua kuwa Mola wako Mlezi ni Mwenye kuwasaidia na kuwanusuru walio hama Makka kukimbiza Dini yao isikandamizwe, na nafsi zao zisiadhibiwe na washirikina. Kisha wakapigana Jihadi kwa kadiri ya uwezo wao, kwa maneno na vitendo, wakavumilia mashaka na taabu, na yaliyo wakuta kwa ajili ya Dini yao. Hakika Mola wako Mlezi baada ya hayo waliyo yastahamia ni Mwenye kuwasamehe wakitubu, Mwenye kuwarehemu, basi hatu wachukulia kwa walio lazimishwa kuyafanya.

111 Ewe Nabii! Watajia watu wako, kwa kuwahadharisha, Siku ambayo kila mtu atakuwa hana linalo mshughulisha ila kujitetea nafsi yake. Hayamshughulishi ya mzazi wala mwana. Siku hiyo ndiyo Siku ya Kiyama! Na Mwenyezi Mungu siku hiyo atailipa kila nafsi malipo ya vitendo iliyo tenda, ikiwa kheri au shari. Na Mola wako Mlezi hamdhulumu hata mtu mmoja.

112 Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* amewapigia mfano watu wa Makka kisa cha mji mmojapo. Watu wake walikuwa wamekaa kwa amani, hawana adui anaye waingilia. Wametua, hawana dhiki ya maisha, riziki inawajia kwa wasaa kutoka kila pahali. Wakazibeua neema za Mwenyezi Mungu, wasimshukuru

113. Na alikwisha wajia Mjumbe wa miongoni mwao wenyewe. Lakini wakamkanusha; basi ili wafika adhabu hali ya kuwa wamedhulumu.¹¹³

114. Basi kuleni katika vile alivyo kupeni Mwenyezi Mungu, vilivyo halali na vizuri. Na shukuruni neema za Mwenyezi Mungu, ikiwa kweli mnamuabudu Yeye.¹¹⁴

115. Amekuharimishieni nyamafu tu, na damu, na nyama ya nguruwe, na mnyama aliye chinjwa kwa ajili isiyo kuwa ya Mwenyezi Mungu. Lakini anaye lazimishwa bila ya kuasi, wala kuruka mipaka, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.¹¹⁵

116. Wala msiseme uwongo, kwa kuropokwa na ndimi zenu: Hichi halali, na hichi haramu - mkimzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Hakika wanao mzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa.¹¹⁶

117. Ni starehe ndogo, nao watapata adhabu chungu.¹¹⁷

118. Na Mayahudi tuliwiharimishia yale tuliyo kuhadithia zamani. Na Sisi hatukuwadhulumu, bali walikuwa wakijudhulumu wenyewe.¹¹⁸

119. Kisha hakika Mola wako Mlezi kwa walio tenda uovu kwa ujinga, kisha wakatubia baada ya hayo na wakatenda mema; bila ya shaka Mola wako Mlezi baada ya hayo ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.¹¹⁹

kwa kumt'ii na kutekeleza amri zake. Mwenyezi Mungu akawatiliza kwa masaibu yaliyo wazunguka kila upande. Wakaonja uchungu wa njaa na vitisho, baada ya utajiri na amani walio kuwa nayo. Na hayo kwa sababu ya kukakamia kwao katika ukafiri na maasi.

113 Nao alikwisha wajia Mtume kutokana nao wenyewe. Ilikuwa ni waajibu wao wamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hayo, lakini walimwambia mwongo, kwa inda na husda tu. Adhabu ikawatwaa nao hali wamo katika udhalimu, na kwa sababu ya hiyo dhulma.

114 Ikiwa washirikina wanazikufuru neema za Mwenyezi Mungu na wanazigeuza kuwa ni nakama, basi nyinyi Waumini elekeeni kwenye shukra. Na kuleni katika alivyo kuruzukuni Mwenyezi Mungu na akakufanyieni kuwa ni vizuri kwenu, wala msijiharimishie nafsi zenu. Na ishukuruni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu kwa kumt'ii Yeye tu peke yake, ikiwa kweli mnamkusudia Yeye tu kwa ibada.

115 Kwani hakika Mwenyezi Mungu hakukuharimishieni isipo kuwa nyamafu, na damu inayo tiririka kutokana na mnyama wakati wa kumchinja, na nyama ya nguruwe, na kilicho chinjwa kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu. Lakini mwenye kulazimishwa na shida ya njaa kula kitu alichokuharimishieni Mwenyezi Mungu, bila ya kutaka, na wala bila ya kupita hadi ya kiasi cha kuondoa ile dharura, basi hakika Mwenyezi Mungu hayachukulii hayo. Kwani Yeye *Subhanahu* ni Mwenye kuwasamehe waja wake. Huwasamehe wanapo tumbukia katika makosa wasio endelea nayo. Naye ni Mwenye kuwarehemu kwa vile anawazuia vitu vinavyo wadhuru, na anawaruhusu kwa kuhifadhi uhai wao.

116 Na ilivyo kuwa Mwenyezi Mungu amekwisha kubainishieni kilicho halali na kilicho haramu, basi shikamaneni na hayo aliyo kubainishieni, wala msithubutu kuhalalisha na kuharimisha ovyo kufuata ndimi zenu. Mkawa mnasema: Hichi halali, na hichi haramu. Matokeo ya hizo kauli zenu ni kumzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na kumkhusisha na asiyo yasema! Hakika wanao mzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawapati kheri wala mafanikio.

117 Wakiendelea kufuata matamano yao ya kidunia, basi hakika starehe yao hiyo ni chache na haina dawamu, na Akhera watapata adhabu kali.

118 Wala hawakuharimishiwa ila Mayahudi tu vile vitu tulivyo kusimulia, ewe Nabii, kabla ya kuteremka Aya hizi. Na vitu hivyo ni kuwa kila mnyama mwenye makucha, na shahamu za ng'ombe na kondoo, ila ilio beba migongo yao au matumbo, au iliyo changanyika na mifupa. Na Sisi hatukuwadhulumu kwa kuwiharimishia hayo, lakini wamejidhulumu wenyewe kuyasabibisha hayo kwa kupita mipaka na ushari wao, na kuacha kusimama kwenye yalio halali.

119 Kisha wanao tenda maovu kwa kupitikiwa, au kwa kuacha kuzingatia vilivyo matokeo yatayo tokea, na baadae wakatubia, wakajitengeneza nafsi zao na vitendo vyao, basi hakika Mola wako Mlezi, ewe Nabii, atawasamehe hao madhambi yao. Kwani hakika Yeye *Subhanahu* baada ya toba hiyo ni Mwingi wa kusamehe madhambi, na ni Mkunjufu wa rehema kwa waja wake.

- 120.** Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.¹²⁰
- 121.** Mwenye kuzishukuru neema zake, Mwenyezi Mungu. Yeye kamteuwa, na akamwongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka.¹²¹
- 122.** Na tukampa wema duniani, na hakika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema.¹²²
- 123.** Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.¹²³
- 124.** Hakika siku ya Sabato (Jumaamosi) waliwekewa wale walio khitalifiana kwa ajili yake. Na hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka atahukumumu baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyo kuwa wakikhitalifiana.¹²⁴
- 125.** Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoka.¹²⁵
- 126.** Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyo adhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanao subiri.¹²⁶

120 Hakika Ibrahim, mnaye tafakhari naye nyinyi washirikina na Mayahudi, alikuwa amekusanya kila fadhila njema, na yu mbali na upotovu wenu, ni mt'iifu wa amri ya Mola wake Mlezi, na wala hakuwa mshirikina kama nyinyi.

121 Alikuwa mwenye kushukuru kwa neema za Mola wake Mlezi. Na kwa haya yote ndio Mwenyezi Mungu alimteua ili abebe Ujumbe wake, na akamwezesha kufuata Njia ya Haki Iliyo Nyooka yenye kufikilia kwenye neema ya kudumu.

122 Na tumemjaalia duniani atajike vyema, na hakika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema wanao neemeshwa kwa Pepo za Allah na radhi zake.

123 Ewe Nabii! Baada ya Ibrahim kwa karne nyingi, tulikupa Wahyi wewe, na tukakuamrisha umfuate Ibrahim katika wito wake wa kulingania Tawhid, na fadhila njema, na kujiepusha na dini za uwongo. Kwani yeye hakuwa katika wanao mshirikisha Mwenyezi Mungu, kama wanavyo msingizia hawa washirikina.

124 Wala sio kuitukuza siku ya Ijuma na kuiacha Jumaamosi kama ilivyo katika Uislamu kuwa ni kukhitalifiana na alivyo kuwa akifanya Ibrahim, kama wanavyo dai Mayahudi. Kwani kuharimishwa kuvua (na kufanya kazi nyengine) siku ya Jumaamosi, ndio Siku ya Sabato, kwa sababu ya kuitukuza haikuwamo katika sharia ya Ibrahim. Hayo walilazimishwa Mayahudi tu (ambao hata hawakuwapo zama za Ibrahim). Na juu ya hivyo hawakuitukuza, bali baadhi yao waliacha kutukuza huko, na wakenda kinyume na amri ya Mola wao Mlezi. Basi yawaje hata wanawatia makosani wengine kwa kutolazimishwa kutukuza jambo ambalo wao walio lazimishwa wameliashi? Ewe Nabii! Kuwa na yakini kuwa Mola wako Mlezi atawahukumumu hao Siku ya Kiyama katika hayo mambo wanayo khitalifiana kwayo, na atamlipa kila mmoja wao kwa vitendo vyake.

125 Ewe Nabii! Lingania, uwite watu kwenye Njia ya Haki ambayo Mola wako Mlezi amewataka watu wako waifuate. Na katika huo Wito wako pita njia ambayo inamnasibu kila mmoja wao. Waite wenye vyeo vya juu katika wao kwa maneno ya hikima kwa mujibu wa akili zao. Na watu wa kawaida walio baki kati yao walinganie kwa kuwapa mawaidha yanao waelekea, na kuwapigia mifano ya mambo wanayo pambana nayo ya kuwapeleka kwenye Haki, na uwaongoze kwenye njia fupi inayo wanasibu. Na jadiliana na watu wa dini zilizo tangulia katika watu wa Biblia, yaani Mayahudi na Wakristo, kwa kutumia hoja za kiakili, Mant'iqi, na maneno laini, na majadiliano mazuri, si maneno ya ukali na matusi, ili uwakinaishe na uwavutie. Hii ndiyo njia ya Daa'wa (Wito), kuwaita watu kumwendea Mwenyezi Mungu -watu wa mila zote. Basi ifuate njia hii unapo waita, na baada ya hayo yaliyo baki mwachilie Mola wako Mlezi, ambaye anamjua aliye zama katika upotovu kati yao na akawa mbali na njia ya uwokovu, na nani ambaye aliye salimika, akaongoka, na akayaamini hayo uliyo waletaa.

126 Enyi Waislamu! Mkitaka kuwaadhibu wale wanao kufanyieni uadui wakakuvamieni, basi waadhibuni kwa kadiri walivyo kutendeeni, wala msizidishe kuliko hivyo. Na kuweni na yakini kwamba mkistahamili,

127. Na subiri. Na kusubiri kwako kusiwe ila kwa sababu ya Mwenyezi Mungu tu. Wala usiwahuzunikie; wala usiwe katika dhiki kwa hila wanazo zifanya.¹²⁷

128. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wenye kumcha, na watendao mema.¹²⁸

msijilipizie kisasi, itakuwa ni kheri zaidi kwenu hapa duniani na Akhera. Basi toeni adhabu kwa ajili ya Haki, wala msiadhibu kwa ajili ya nafsi zenu.

127 Na ewe Nabii! Subiri! Kwani hivyo ndio yatakusahilikia mengi katika mashaka ya maisha, na yataondoka matatizo yake. Wala usisikitike kwa kuwa watu wako hawaitikii Wito wako, na hawakuamini. Wala usione dhiki kifuaani mwako kwa hila zao na vitimbi vyao vya kuukaba roho Wito wako. Kwani vitendo vyao havitakudhuru kitu. Na wewe umekwisha tekeleza waajibu wako, na umemcha Mola wako Mlezi.

128 Kwani hakika Mola wako Mlezi yu pamoja na wale wanao jikinga na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kuyaepuka anayo yakataza, na wakazifanya a'mali zao ziwe nzuri kwa sababu ya Mwenyezi Mungu kwa kukubali kumt'ii. Yeye atawanusuru duniani, na Akhera atawalipa bora ya malipo.

Sura 17 - Al-Israa (Bani Israil)

Utangulizi

Sura hii tukufu ina Aya 111, nayo ni Sura ya Makka ila Aya hizi: 26, 32, 33, 57 na tangu Aya 73 mpaka Aya 80. Aya zote hizi, nazo ni 12, ni za Madina. Sura hii imeanza kwa kumsabihi, kumtakasa, Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kisha ikaitaja Israi, nayo ni safari ya usiku aliye chukuliwa Mtume s.a.w. kutoka Makka mpaka Bait Al Muqaddas (Yerusalemu), na baadae akapelekwa mbinguni, na kurejeshwa Makka usiku ule ule. Baadae Sura inaeleza Ujumbe wa Nabii Musa a.s., na yaliyo kuwa ya Wana wa Israili. Kisha ikaashiria cheo cha Qur'ani Tukufu katika uwongofu, na zikatajwa Aya za uumbaji usiku na mchana, na yatakayo watokea watu Siku ya Kiyama katika kulipwa kwa vitendo walivyo vitenda duniani. Na *Subhanahu* amebainisha sababu za kuharibika umma, na hali ya watu katika kuhangaika kwao, na matokeo ya vitendo vyao huko Akhera. Tena zikaja Aya za kutukuzwa wazazi, baba na mama, na hali ya watu kukhusu mali zao; na zikaja Amri Kumi za kuunda umma ulio bora. Kisha *Subhanahu* akauvunja uzushi wa washirikina kukhusu Malaika, kisha akabainisha Qur'ani inavyo eleza hoja zake.

Kisha *Subhanahu* akaashiria anavyo stahiki kuhimidiwa, na upinzani wa washirikina, akawapa wasia Waumini. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu akaeleza namna anavyo watendea makafiri duniani na Akhera. Tena akaeleza asili ya uumbaji wa binaadamu na Shet'ani, na akawatisha washirikina kwa Aya zake. Baada ya hayo *Subhanahu* alibainisha utukufu wa binaadamu, na akataja adhabu za Siku ya Kiyama. Akataja vipi washirikina wanavyo jaribu kumzuia Nabii asitimize Wito wake, na vipi Mwenyezi Mungu anavyo mtia nguvu. Baada ya hayo Allahu *Subhanahu wa Taa'la* akamuusia Nabii kwa wasia za uwongofu, na wito mnasaba. Kisha akaashiria cheo cha Qur'ani Tukufu, na akataja khabari za Roho, na akaashiria siri zake. Kisha akataja umuujiza wa Qur'ani, kushindwa majini na watu kuleta mfano wake. Na akabainisha *Subhanahu* uwezo wake kuleta Ishara nyengine. Tena akataja vipi Qur'ani ilivyo kusanya Haki, na hali za Waumini wema katika Imani zao, na inavyo takikana kuwa daima wawe wanamhimidi Mwenyezi Mungu na wakimtukuza.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. *SUBHANA*, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.¹

1 Mwenyezi Mungu aliye takasika na kila ambalo lisio laiki naye. Yeye ndiye aliye mchukua mja wake Muhammad wakati wa usiku kutoka Msikiti Mtakatifu wa Makka kwendea Msikiti wa Mbali wa Baitul Muqaddas, ambao tuliwabarikia wakaazi majirani wa Msikiti huo katika mahitaji yao, ili tumwonyeshe baadhi ya Ishara zetu zenye ushahidi wa kutosha wa kuthibitisha kuwa Mimi ni Mungu Mmoja peke yangu, na ukubwa wa uwezo wangu! Hakika Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kuona.

2. Na tukampa Musa Kitabu, na tukakifanya uwongofu kwa Wana wa Israili. (Tukawambia): Msiwe na mtegemewa ila Mimi!²
3. Enyi kizazi tuliyo wachukua pamoja na Nuhu! Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani.³
4. Na tukawahukumia Wana wa Israili katika Kitabu kwamba: Hakika nyinyi mtafanya fisadi katika nchi mara mbili, na kwa yakini mtapanda kiburi, kiburi kikubwa.⁴
5. Basi itapo fika ahadi ya kwanza yake tutakupelekeeni waja wetu wa kali kwa vita. Watakuingilieni ndani ya majumba. Na hii ilikuwa ahadi iliyo timizwa.⁵
6. Kisha tukakurudishieni nguvu zenu dhidi yao, na tukakusaidieni kwa mali na wana, na tukakujaalieni mkawa wengi zaidi.⁶
7. Basi mkifanya wema, mnajifanyia wema nafsi zenu. Na mkifanya ubaya, mnajifanyia wenyewe. Na ikifika ahadi ya mwisho ili waziharibu nyuso zenu, na waingie Msikitini kama walivyo ingia mara ya kwanza, na waharibu kila walicho kiteka kwa uharibifu mkubwa.⁷
8. Huenda Mola wenu Mlezi akakurehemuni. Na mkirudia na Sisi tutarudia. Na tumeifanya Jahannamu kuwa ni gereza kwa ajili ya makafiri.⁸
9. Hakika hii Qur'ani inaongoa kwenye ya yaliyo nyooka kabisa, na inawabashiria Waumini ambao wanatenda mema ya kwamba watapata malipo makubwa.⁹

2 Na hakika hiyo Baitul Muqaddas ilikuwa inakaliwa na Wana wa Israili baada ya Musa, mpaka walipo fanya fisadi yao humo, wakafukuzwa hapo zamani. Haya ijapo kuwa Sisi tulimpa Musa Taurati, na tukatia ndani yake uwongofu, na tukawaambia: Msimfanye yeyote wa kumtegemezea mambo yenu isipo kuwa Mwenyezi Mungu.

3 Nyinyi Wana wa Israili mmezalikana kutokana na wale watu safi wema walio kuwa na Nuhu katika safina baada ya kuwa wameamini. Nasi tukawaokoa wasizame. Basi mfanyeni Nuhu kuwa ndiye mwongozi wenu wa kumfuata, kama walivyo mfanya wazee wenu walio tangulia. Kwani hakika yeye alikuwa mja wa wingi wa shukrani kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake.

4 Na tukatekeleza hukumu yetu kwa Wana wa Israili katika tuliyo yaandika katika *Lauhun Mahfuudh*, Ubao Ulio Hifadhiwa, ya kwamba watafanya ufisadi katika Nyumba Takatifu (Baitul Muqaddas) bila ya shaka yoyote mara mbili. Kila mara katika hizo itakuwa ni udhaalimu na uasi, na kuacha hukumu za Taurati, na kuwauwa Manabii, na mtasaidiana katika madhambi, na kwamba utawala wenu utaenea, na kutukuka na kupanda kichwa na kiburi kwa dhulma zenu.

5 Na ulipo fika wakati wa kukuleteeni adhabu mara ya kwanza, tulikupatilizeni, kwa sababu ya fisadi yenu, kwa kukusalitishieni watu wa kali kupigana. Wakakingilieni mpaka ndani ya majumba, hapana walicho kiacha, ili wakuuweni. Na ahadi ya kukuadhibuni ilikuwa ni ahadi haina budi kutimizwa.

6 Kisha mambo yenu yalipo kaa sawa, na mkaongoka, na mkatengeneza umoja wenu, na mkaacha ufisadi, tukakurejezeeni ushindi juu ya wale makhasimu zenu. Nasi tukakuruzukuni mali na wana, na mkazidi kuwa wingi kwa idadi.

7 Na tukawambia: Mkifanya wema na mkamt'ii Mwenyezi Mungu, wema wenu utakufaeni nafsi zenu duniani na Akhera. Na mkifanya uovu kwa maasi, basi mnajiharibia nafsi zenu vile vile. Na utapo kuja wakati wa adhabu pale mara ya mwisho katika zile mara mbili za ufisadi wenu katika nchi, tutakupelekeeni maadui zenu, wafanye athari za uovu na madhila na huzuni zidhihiri nyusoni mwenu. Na matokeo yake ni kuingia katika Msikiti wa Baitul Muqaddas, wakauharibu kama walivyo ingia na wakauharibu mara ya kwanza, wakateketeza watacho kipata kwa uteketezi mkubwa.

8 Asaa Mola wenu Mlezi akakurehemuni baada ya hiyo mara ya pili pindi mkitubu. Na mkirejea kwenye ufisadi Nasi tutarejea kukuadhibuni. Na tumeifanya Jahannam kuwa ndiyo gereza la kuwafungia makafiri!

9 Hakika hii Qur'ani inawaongoza watu kwenye njia ambayo ndiyo njia iliyo kaa sawa kabisa kuliko njia zote, na ndiyo njia ya salama kabisa ya kufikilia kwenye furaha ya kweli katika dunia. Na wabashirie wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wenye kuit'ii Haki na wanatenda vitendo vyema, kuwa watapata ujira mkubwa Siku ya Kiyama.

10. Na yakwamba wale wasio iamini Akhera tumewaandalia adhabu chungu.¹⁰
11. Na mwanaadamu huomba shari kama vile aombavyo kheri, kwani mwanaadamu ni mwenye pupa.¹¹
12. Na tumefanya usiku na mchana kuwa ishara mbili. Tena tukaifuta ishara ya usiku, na tukaifanya ishara ya mchana ni yenye mwangaza ili mtafute fadhila itokayo kwa Mola wenu Mlezi, na mpate kujua idadi ya miaka na hisabu. Na kila kitu tumekifafanua waziwazi.¹²
13. Na kila mtu tumemfungia a'mali yake shingoni mwake. Na Siku ya Kiyama tutamtotea kitabu atakacho kikuta kiwazi kimekunjuliwa.¹³
14. Ataambiwa: Soma kitabu chako! Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu.¹⁴
15. Anaye ongoka basi anaongoka kwa ajili ya nafsi yake. Na anaye potea basi anapotea kwa khasara yake mwenyewe. Wala habebi mbebaji mzigo wa mwengine. Wala Sisi hatuadhibu mpaka tumeleke Mtume.¹⁵
16. Na pindi tukitaka kuuteketeza mji huwaamrisha wale wenye starehe na taanusi, lakini wao huendelea kutenda maovu humo. Basi hapo kauli huthibiti juu ya mji huo, nasi tukauangamiza kwa maangamizo makubwa.¹⁶
17. Na kaumu ngapi tumeziangamiza baada ya Nuhu! Na Mola wako Mlezi anatosha kabisa kuwa ni Mwenye kuzijua na kuziona dhambi za waja wake.¹⁷
18. Anaye taka yapitayo upesi upesi, tutafanya haraka kumletea hapa hapa tunayo yataka kwa tumtakaye. Kisha tumemwekea Jahannamu; ataingia humo hali ya kuwa

10 Na hakika wale ambao hawaiamini Akhera tumewatengenezea adhabu ya machungu makali.

11 Ni katika tabia ya mwanaadamu kufanya haraka katika kuwahukumia watu kwa yanayo wapata, na katika kauli zake na vitendo vyake. Naye hukimbilia kulingania shari kama anavyo lingania kheri. Naye hufanya haraka kumuapiza kwa Mwenyezi Mungu amteremshia shari yule aliye mkasirisha, kama anavyo fanya haraka kuomba kheri.

12 Na Sisi tumejaalia usiku na mchana, kwa namna yao na kupishana kwao, kuwa ni alama zenye kuonyesha Upweke wetu na Uwezo wetu. Tukauondoa mwangaza kwenye usiku, na kisionekane kitu. Na alama yake ni giza liso kuwa na jua. Hiyo ni ishara kubwa. Na mchana tukaufanya wa kuangaza. Hapo laonekana jua, ile ishara kuu, ili mpate kwenda mtakako wakati huo katika kutafuta maisha yenu. Na katika kuja usiku na mchana mpate kujua idadi ya miaka na hisabu za miezi na siku. Na Sisi tumekubainishieni kila kitu kwa uwazi kwa sababu ya maslahi yenu, ili isimame hoja juu yenu baada kutimia neema.

13 Na kila mtu tumemfungamanisha na a'mali yake, vitendo vyake, kama koja lilioko shingoni. Na Siku ya Kiyama tutamtotea kitabu kilicho andikwa vitendo vyake vyote. Atakiona kitabu hicho kiwazi iwe wepesi kwake kukisoma.

14 Ataambiwa: Soma kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa duniani alikuwa hajui kusoma. Soma kitabu cha a'mali zako. Hicho leo kinatosha kukuhisabia na kukudhibitia vitendo vyako.

15 Mwenye kufuata njia ya Haki basi anajifaa mwenyewe, na mwenye kuiacha basi anajipoteza mwenyewe. Wala hapana mwenye kubeba dhambi zake akambebea dhambi za mwengine. Wala haitufalii kumuadhibu yeyote kwa kutenda kitu kabla hatujampelekea Mtume kutoka kwetu amwonyeshe njia ya Haki na kumkataza maovu.

16 Na pindi tukikadiria tangu azali katika *Lauhun-mahfuudh* kuwateketeza watu wa mji fulani kwa mujibu wa hikima yetu, basi Sisi huwasalitisha wale walio jidekeza kwa taanusi katika huo mji, wakafanya fisadi zao, wakaacha njia ya Haki, na wakawafuata wengine bila ya kutambua, na kwa hivyo huo mji wote tena hapo hustahiki kuangamizwa. Nasi huuangamiza vikubwa mno!

17 Na kaumu nyingi zilizo kuja baada ya Nuhu tuliziangamiza kwa kuwaasi Manabii wao. Na yakutosha kuwa ni ishara ya Mola wako Mlezi kwamba Yeye ni Mjuzi wa kila kitu kama kilivyo, kwa ujuzi wa Mwenye kuona. Naye anazo khabari za dhambi za waja wake, na Mwenye kuziona. Hapana chochote katika vitendo vya waja wake asicho kijua, na Yeye atawalipa kama wanavyo stahiki.

ni mwenye kulaumiwa na kufurushwa.¹⁸

19. Na anaye itaka Akhera, na akazifanyia juhudi a'mali zake, naye ni Muumini, basi hao juhudi yao itakuwa ni ya kushukuriwa.¹⁹

20. Wote hao tunawakunjulia - hawa na hao - katika neema za Mola wako Mlezi. Wala neema za Mola wako Mlezi hazizuiliki.²⁰

21. Angalia vipi tulivyo wafadhili baadhi yao kuliko wengine. Na hakika Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na fadhila kubwa zaidi.²¹

22. Usimfanye mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu, usije ukawa wa kulaumiwa uliye tupika.²²

23. Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemu wa hishima.²³

24. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyo nilea utotoni.²⁴

25. Mola wenu anajua kabisa yaliyo nyoyoni mwenu. Ikiwa nyinyi mtakuwa wema, basi hakika Yeye ni Mwenye kuwaghufiria wanao tubia kwake.²⁵

26. Na mpe aliye jamaa yako haki yake, na masikini, na msafiri; wala usitumie ovyo kwa fujo.²⁶

18 Mwenye kutaka starehe za dunia hii ipitayo na akazitumikia kwa kutafutia kisingizio, wala asiwe na yakini na miadi, na wala asingojee malipo ya Akhera, tutamletea haraka haraka tuyatakayo ya duniani kwa ukunjufu na wasaa. Haya ni kwa tumtakaye kumletea haraka. Kisha tutamuandalia kwa Akhera Jahannamu ahilikike kwa joto lake, naye hali awe ni mwenye kushutumiwa kwa aliyo yatenda, mwenye kutengwa mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu.

19 Na mwenye kuitaka Akhera kwa vitendo vyake, naye akawa navyo hivyo vitendo, na akawa anamuamini Mwenyezi Mungu na malipo yake, basi watu kama hao vitendo vyao vitakubaliwa na Mwenyezi Mungu na watapata malipo kwa ajili yake.

20 Na Sisi tutawakunjulia neema za Mola wako Mlezi hapa duniani makundi yote mawili, pindi wakichukua khatua ya kufikia hayo. Wala neema za Mola wako Mlezi hatonyimwa yeyote, akiwa Muumini au akiwa kafiri, maadamu wakishika njia za kuzitafuta.

21 Hebu angalia kwa kuzingatia vipi tulivyo wafadhilisha baadhi ya waja wetu kuliko wengine, kwa kuwapa mali na vyeo na nafasi, pindi wakishika njia za kuyapata hayo katika dunia. Na hayo ni kwa hikima tunayo ijua Sisi. Na tafauti zao katika Akhera ni kubwa zaidi kuliko tafauti zao za duniani. Kwa hivyo yatafikana waishughulikie Akhera, kwani huko ndiko kwenye kutukuka kwa kweli na kuzidiana kwa hakika.

22 Ewe mwenye jukumu! Usimfanye Mwenyezi Mungu kuwa na mshirika, utakuja fedheheka kwa kudharauliwa, na utajaaliwa uwe mwenye kutupika.

23 Na Mola wako Mlezi amehukumu kuwa msimuabudu yeyote isipo kuwa Yeye. Na pia muwafanyie wema kwa ukamilifu wazazi wenu wawili. Na hao, au mmoja wao, wakifikilia kwako hali ya unyonge na mwisho wa umri wao, basi lisikutoke tamko la kuchoka nao au kuudhika kwa yanayo kupata kutokana nao. Wala usiwahamatie. Na nena nao maneno mazuri, laini, yenye kuwaonyesha ihsani na kuwahishimu.

24 Na wafanyie upole, na wanyenyekee kwa kuwaonea huruma, na uwaombe: Ewe Mola Mlezi! Warehemu wote wawili, kama walivyo nifanyia huruma walipo nilea utotoni.

25 Enyi watu! Mola wenu Mlezi anajua kuliko nyinyi yaliyomo katika dhamiri zenu, na atakuhasibuni kwayo kwa thawabu na i'kabu. Na mkiwa mnakusudia wema na mkautenda, tena mkatokea baadhi yenu mkateleza, na kisha mkarejea kwa Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu *Subhanahu* atakusameheni. Kwani Yeye ni Mwenye kusamehe daima kwa wale wanao rejea kwake.

26 Na wape jamaa zako haki yao kwa kuwafanyia wema na kuwaunga; na kadhaalika masikini mwenye haja, na msafiri aliye katikana na mali yake. Wape hao haki yao katika Zaka na sadaka, wala usiyavuruge mali yako kwa utumiaji ovyo usio na maslaha.

27. Hakika wabakhirifu ni ndugu wa Mashet'ani. Na Shet'ani ni mwenye kumkufuru Mola wake Mlezi.²⁷
28. Na ikiwa unajikurupusha nao, nawe unatafuta rehema ya Mola wako Mlezi unayo itaraji, basi sema nao maneno laini.²⁸
29. Wala usiufanye mkono wako kama ulio fungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa mufisi.²⁹
30. Hakika Mola wako Mlezi humkunjulia riziki amtakaye, na humpimia amtakaye. Hakika Yeye kwa waja wake ni Mwenye kuwajua na kuwaona.³⁰
31. Wala msiwauwe wana wenu kwa kuogopa umasikini. Sisi tunawaruzuku wao na nyinyi. Hakika kuwau hao ni khatia kubwa.³¹
32. Wala msikaribie uzinzi. Hakika huo ni uchafu na njia mbaya.³²
33. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu amekataza isipo kuwa kwa haki. Na aliye uliwa kwa kudhulumiwa basi tumempa madaraka mrithi wake. Lakini asipite mpaka katika kuuwa. Kwani yeye anasaidiwa.³³
34. Wala msiyakaribie mali ya yatima, isipo kuwa kwa njia iliyo bora, mpaka afike utuuzimani. Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itasailiwa.³⁴
35. Na timizeni kipimo mpimapo. Na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na khatimaye ndio bora.³⁵

27 Kwani wabakhirifu (watumiaji ovyo) wenzao ni Mashetani, wanapokea minong'ono yao wanapo wachochea wafanye ufasidi na watumie kwa uharibifu. Na ni mtindo wa Shetani daima kukufuru neema ya Mola wake Mlezi. Na sahibu yake ni hali kadhaalika.

28 Ukilazimika kujikurupusha na hao walio tajwa wenye haja, kwa sababu ya shida uliyo nayo, na ukawa hukuwapa kwa kuto kuwa nacho cha kuwapa sasa, na ilhali unataraji Mwenyezi Mungu atakufungulia baadae, basi nena nao kwa maneno mema ya kuwapa imani nawe.

29 Wala usiuzulie mkono wako kutoa katika mambo ya kheri, ukaufanya kama ulio fungwa pingu za chuma shingoni mwako ukawa huwezi kuukunjua. Wala usiukunjue wote kabisa kwa kutumia ovyo. Utakuja tukanika kwa ubakhili na majuto, au utabaki huna kitu umefilisika kwa sababu ya ubadhirifu na israfu.

30 Hakika Mola wako Mlezi humkunjulia riziki amtakaye katika waja wake, na humdhikisha katika wao amtakaye. Kwani Yeye anawajua vyema tabia zao, na anazona hali zao. Basi Yeye humpa kila mmoja wao, pindi akishika njia zake, kwa inavyo wafikiana na hikima yake Mwenyezi Mungu.

31 Ikiwa yaliyo khusiana na riziki yamo mikononi mwa Mwenyezi Mungu, basi haikufaliini kuwauwa watoto wenu kwa kukhofu ufakiri utao weza kutokea. Kwani Sisi ni Wenye kudhamini riziki zao na riziki zenu. Hakika kuwau hao ni dhambi kubwa.

32 Wala msiukaribie uzinzi, kwa kuziingilia sababu zinazo pelekea uzinzi. Jambo hilo ni jambo la aibu na uovu usio fichikana, na hapana njia mbovu kama hiyo.

33 Wala msiuwe nafsi yoyote ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa ila kuuwa huko kukiwa kwa haki, kwa kuwa nafsi hiyo inastahiki kuuwawa kwa ajili ya kisasi au kuwa ni adhabu ya sharia. Na mwenye kuuliwa kwa kudhulumiwa Sisi tumempa jamaa yake wa karibu haki juu ya yule muuwaji, kwa kutaka kwa Qadhi auliwe kwa kisasi. Lakini naye asipite mpaka katika kuuwa, akataka kumuwa mtu mwengine asiye kuwa muuwaji, au kwa kuwauwa wawili badala ya mmoja. Kwani Mwenyezi Mungu amemsaidia huyo kwa kumpa haki ya kisasi au kulipwa fidiya. Basi haimfali kukiuka mipaka iliyo wekwa.

34 Wala msiyatumie mali ya yatima ila kwa njia iliyo bora kabisa, ya kuamirisha na kuikuza. Na endeleeni hivyo mpaka huyo mtoto afike umri wa utambuzi kuweza kuendesha mambo yake. Na akisha fika hivyo basi mkabidhini mali yake, na timizeni ahadi zote mlizo chukua. Kwani Mwenyezi Mungu atamsaili aliye vunja ahadi kwa kuvunja kwake, na atamhisabia kwa hayo..

35 Na mnapo mpimia mushtiri mpimieni vilivyo, na pimeni mizani kwa uadilifu. Kwani kuweka sawa vipimo na mizani ni bora kwenu kwa hapa duniani, kwa sababu huwaraghibisha watu kufanya nanyi biashara. Na malipo mazuri zaidi ni ya Akhera.

36. Wala usiyafuate usiyo na ujuzi nayo. Hakika masikio, na macho, na moyo - hivyo vyote vitasailiwa.³⁶
37. Wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima.³⁷
38. Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza kwa Mola wako Mlezi.³⁸
39. Haya ni katika hikima alizo kufunulia Mola wako Mlezi. Wala usimweke pamoja na Mwenyezi Mungu mungu mwengine, usije ukatupwa katika Jahannamu ukilaumiwa na kufurushwa.³⁹
40. Je! Mola wenu Mlezi amekuteulieni wavulana, na Yeye akawafanya Malaika ni banati zake? Kwa hakika nyinyi mnasema usemi mkubwa.⁴⁰
41. Na tumekwisha bainisha katika Qur'ani hii ili wapate kukumbuka. Lakini haikuwazidisha ila kuwa mbali nayo.⁴¹
42. Sema: Lau kuwa wangeli kuwa pamoja naye miungu mingine kama wasemavyo, basi wangeli tafuta njia ya kumfikia Mwenye Kiti cha Enzi.⁴²
43. *Subhanahu Wa Taa'la*, Ametakasika na Ametukuka juu kabisa na hayo wanayo yasema.⁴³
44. Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye maghfira.⁴⁴
45. Na unapo soma Qur'ani tunaweka baina yako na wale wasio iamini Akhera pazia

36 Ewe mtu! Usifuate maneno wala vitendo usivyo vijua. Basi usiseme: Nimesikia...na hali hukusikia. Au: Najua...na hali hujui. Kwani masikio, macho na moyo, vyote hivyo Siku ya Kiyama vitamuuliza mtu kwa alivyo tenda kwavyo.

37 Wala usitembee katika ardhi kwa kiburi na majivuno. Kwani vyovyote utavyo fanya huwezi kuipasua ardhi kwa nguvu za mkanyago wako, na kama utavyo kuwa mrefu huwezi kuipita urefu milima.

38 Yote hayo yaliyo tajwa katika mausio ni mambo mabaya yaliyo katazwa na yanayo chusha na kuchukiza kwa Mola wako Mlezi.

39 Na hayo ni katika aliyo kufunulia Mola wako Mlezi, katika kuijua haki kwa dharti yake, na kheri ipate kutendwa. Wala usimfanyie Mwenyezi Mungu kuwa na mungu mwengine, usije kutupwa katika Jahannamu ukijilaumu na ukilaumiwa, umeangamia na umefurushwa mbali na rehema za Mola wako Mlezi.

40 *Subhanahu* anayachukia wayasemayo makafiri kwamba Malaika ni mabinti wa Mwenyezi Mungu. Anasema: Mola wenu Mlezi amekufadhilisheni kuliko Mwenyewe kwa kukupeni nyinyi watoto wanaume wenye nguvu, na Yeye akawafanya Malaika ni banati zake kwa mnavyo dai? Kwa maneno yenu haya mnazua matusi makubwa.

41 Sisi tumebainisha katika Qur'ani hii kwa uwazi mzuri, tukipiga mifano na kutoa mawaidha na hukumu, ili wapate kuwaidhika hawa washirikina. Lakini nyoyo zao zimekuwa kama mawe. Kubainisha huku hakukuwazidishia ila kuzidi kuwakimbiza na Haki.

42 Ewe Nabii! Ili kudhihirisha upotovu wa madai yao wanao mshirikisha Mwenyezi Mungu, sema: Lau kuwa wapo miungu wengine pamoja na Mwenyezi Mungu kama wasemavyo, hao miungu wangeli tafuta njia kumfikilia huyo Mwenye Ufalme wa mwisho ili wapate kushindana naye.

43 Mwenyezi Mungu ametakasika kabisa kama anavyo stahiki, na ametukuka aliye mkuu shani yake na yote wanayo dai kuwa wapo pamoja na Yeye miungu wengine.

44 Hakika mbingu saba na ardhi, na viumbe vyote viliomo humo, vinamtakasa na kumtukuzi, na vinaonyesha uzuri wa kuumba kwake, na kutakasika kwake *Subhanahu* na kila upungufu, na kukamilika ufalme wake, na kwamba Yeye hana mshirika na yeyote katika viumbe wa Ufalme wake uliyo enea. Vyote hivyo vinamtakasa na kumsifu. Lakini makafiri hawafahamu hoja hizi kwa kutawaliwa nyoyo zao na mghafala. Na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwao, na Mwenye kuwasamehe wanao tubu. Kwa hivyo hawafanyii haraka kuwapa adhabu.

linalo wafunika.⁴⁵

46. Na tunaweka vifuniko juu ya nyoyo zao wasije wakaifahamu, na tunaweka kwenye masikio yao uziwi. Na unapo mtaja katika Qur'ani Mola wako Mlezi peke yake, basi wao hugeuka nyuma wakenda zao.⁴⁶

47. Sisi tunajua vyema kabisa sababu wanayo sikilizia wanapo kusikiliza, na wanapo nong'ona. Wanapo sema hao madhaalimu: Nyinyi hamumfuati isipo kuwa mtu aliye rogwa.⁴⁷

48. Tazama vipi wanavyo kupigia mifano. Basi wamepotea. Kwa hivyo hawawezi kuipata njia.⁴⁸

49. Na walisema: Je! Tutapo kuwa mifupa na mapande yaliyo vurugika, tutafufuliwa kwa umbo jipya?⁴⁹

50. Sema: Kuweni hata mawe na chuma.⁵⁰

51. Au umbo lolote mnalo liona kubwa katika vifua vyenu. Watasema: Nani atakaye turudisha tena? Sema: Yule yule aliye kuumbeni mara ya kwanza! Watakutikisia vichwa vyao, na watasema: Lini hayo? Sema: A'saa yakawa karibu!⁵¹

52. Siku atakapo kuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru, na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mdogo tu.⁵²

53. Waambie waja wangu waseme maneno mazuri, maana Shet'ani huchochea ugomvi baina yao. Hakika Shet'ani ni adui aliye dhaahiri kwa mwanaadamu.⁵³

54. Mola wenu Mlezi anakujueni vilivyo. Akipenda atakurehemuni, na akipenda atakuadhibuni. Na hatukukutuma ili uwe mlinzi juu yao.⁵⁴

45 Ewe Nabii! Unapo soma Qur'ani inayo taja dalili za Haki, Sisi huweka pazia, lenye kukuficha baina yako na wale wasio amini kufufuliwa na malipo, pale wanapo taka kukushambulia. Kwa hivyo hawakuoni.

46 Na kwa mujibu wa hikima yetu ya kupotoa na kuongoa huweka vifuniko juu ya nyoyo zao, wasipate kuifahamu Qur'ani ilivyo. Na katika masikio yao hutia uziwi basi hawasikii lenye manufaa kwao. Hayo ni kwa sababu ya kupindukia katika inda yao na majivuno yao. Na pale unapo mtaja Mola wako Mlezi katika Qur'ani peke yake bila ya kuwataja miungu yao, wao basi hurejea nyuma wakaacha kukusikiliza.

47 Sisi tunajua vyema vile wanavyo isikiliza Qur'ani nao ilhali wanaikejeli na kuifanyia maskhara na huku wanakusikiliza. Nao wanayaficha yaliyo semwa. Na hiyo ndiyo kauli ya wenye kudhulumu katika siri zao, wakisema: Ikiwa mtamfuata huyu basi hamumfuati ila mtu aliye geuzwa akili yake.

48 Hebu angalia vipi walivyo kushabihisha; wamekushabihisha na mtu aliye rogwa, na wakakuita kohani, mtunga mashairi, wakaipotea njia ya hoja. Kwa hivyo wasiweze kupata njia ya kuzua tusi linalo kubalika, au kwa hivyo wakaukosa uwongofu, na wasiipate njia ya kuufikilia.

49 Wanao kataa kuwa watafufuliwa wanasema: Hivyo tutafuliwa baada ya kwisha kuwa mafupa yaliyo bunguliwa, na mapande mbali mbali, tukawa hai na umbo jipya? Haya hayaingii akilini.

50 Ewe Nabii! Waambie: Hata mkiwa mawe yasiyo na uhai, au chuma, ambacho ni kigumu kuliko jiwe, 51 Au umbo jingeneo lolote ambalo mnaona kwa mawazo yenu haliwezi kuwa hai, basi hapana shaka yoyote mtafufuliwa! Watasema kwa kuona ni muhali: Nani atakaye turejesha hivyo? Waambie: Atakurjesheni Mwenyezi Mungu, yule yule aliye kuumbeni mara ya kwanza. Watakutikisia vichwa vyao kwa mastaajabu, nao wakisema kwa kejeli: Huko kufufuliwa unako tuahidi kutakuwa lini? Waambie: Nataraji kutakuwa karibu!

52 Na siku atapo kufufueni Mwenyezi Mungu kutoka makaburini kwenu, mtafufuliwa nanyi mkimshukuru na kumsifu Mola wenu Mlezi kwa ukamilifu wa uwezo wake. Na mtadhani kuwa hamkukaa makaburini kwenu ila muda mchache tu. Mtaona muda ni mfupi kwa mnasaba ya hayo mnayo yaendea.

53 Ewe Nabii! Waambie waja wangu Waumini wanapo pambana na washirikina waseme maneno yaliyo bora ya kukinaisha, na waachilie mbali kutumia maneno makali makali yanayo sabibisha shari na uharibifu. Kwani Shetani huleta fisadi baina ya Waumini na makafiri, kwa kuwa yeye ni adui aliye wazi wa binaadamu.

54 Mola wenu Mlezi ndiye anaye jua vyema mwisho wa mambo yenu. Akipenda atakurehemuni kwa

- 55.** Na Mola wako Mlezi anawajua vilivyo waliomo mbinguni na katika ardhi. Na hakika tumewafadhilisha baadhi ya Manabii kuliko wengine; na Daudi tulimpa Zaburi.⁵⁵
- 56.** Sema: Waombeni hao mnao wadaia badala yake Yeye. Hawawezi kukuondoleeni madhara, wala kuyaweka pengine.⁵⁶
- 57.** Hao wanao waomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kwenda kwa Mola wao Mlezi - hata miongoni mwao walio karibu mno - na wanataraji rehema zake na wanaikhofu adhabu yake. Hakika adhabu ya Mola wako Mlezi yafaa kutahadhari nayo.⁵⁷
- 58.** Na hapana mji wowote ila Sisi tutauteketeza kabla ya Siku ya Kiyama, au tutaupa adhabu kali. Haya yamekwisha andikwa katika Kitabu.⁵⁸
- 59.** Na hapana kinacho tuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha. Na tuliwapa Wathamudi ngamia jike kuwa ni Ishara iliyo dhaahiri, lakini walidhulumu kwaye. Nasi hatupeleki Ishara ila kwa ajili ya kuhadharisha.⁵⁹
- 60.** Na tulipo kwambia: Hakika Mola wako Mlezi amekwisha wazunguka hao watu. Na hatukuifanya ndoto tulio kuonyesha ila ni kuwajaribu watu, na mti ulio laaniwa katika Qur'ani. Na tunawahadharisha, lakini haiwazidishii ila uasi mkubwa.⁶⁰

kukupeni tawfiki ya Imani, (uwezo wa kuamini) au akipenda atakupeni adhabu kwa kuikosa hiyo Imani. Wala Sisi hatukukupeleka wewe uwe ni mwakilishi wao kwa mambo yao, hata uwalazimishe kuamini. Bali tumekutuma uwe ni mbashiri kuwapa khabari njema wenye kusadiki, na mwonyaji kuwaonya wanao kanusha. Waachilie mbali, na waamrishe sahaba zako wawastahamilie.

55 Na Mola wako Mlezi anajua vilivyo vyote viliomo mbinguni na ardhini, na anajua hali zao. Basi anawakhiari miongoni mwao kwa kuwapa Unabii awatakao. Naye amekukhiari wewe kwa kukupa Utume wake. Basi haiwafalii wao kuudhika na Unabii wako. Na hao Manabii si wote sawa sawa kwa daraja mbele yake Aliye tukuka shani yake. Bali baadhi yao ni bora kuliko wengine. Naye amewatukuza baadhi ya Manabii juu ya wengine kwa miujiza, na wingi wa wafwasi, si kwa ufalme. Basi alitukuzwa Daudi kwa kuwa kapewa Zaburi, si kwa kuwa kapewa ufalme. Basi hapana ajabu kuwa wewe, Muhammad, ukapata fadhila kubwa kabisa kwa kuwa umepewa Qur'ani.

56 Waambie hawa wanao abudu viumbe na wanadai kuwa hao ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu: Waombeni hao mnao waabudu inapo kuteremkieni shida, au mkakhofu kuwa itakushukieni. Hamtopata kwao chochote cha kukuondoleeni madhara yenu, wala kuyahamisha akapewa mwinginewe.

57 Na hakika hawa viumbe wanao waomba wale wanao waabudu, wao wenyewe wanamuabudu Mwenyezi Mungu, na wanaomba wapate daraja na cheo kwake kwa ut'iifu, na wana pupa ya kutaka wawe karibu zaidi na Mwenyezi Mungu, na wanatumaini kupata kwake rehema, na wanaikhofu adhabu yake. Hakika adhabu ya Mwenyezi Mungu inatakikana kutahadhari nayo na kuiogopa!

58 Na ni mazoea yetu kuuteketeza kila mji na watu wake unapo dhulumu mji huo. Au huwapa adhabu kali watu wake kwa mauwaji au vyenginevyo. Basi watu wako watahadhari, kwani hukumu yetu imekwisha hukumiwa, na imekwisha andikwa katika Kitabu chetu.

59 Watu wako wamekutaka uwalettee Ishara na miujiza. Nao hawakukinaika kwa yaliyo wajia ambayo huwakinaisha wenye akili. Na mwendo wetu umekwisha wapitia hao wanao taka miujiza, na wanapo kubaliwa wasiamini, nao ni kuwang'olea mbali kwa adhabu kama tulivyo wafanyia wa kale. Miongoni mwa hao ni watu wa Thamud. Walitaka miujiza, akawa ngamia mke ni muujiza wazi kwao wa kuondoa shaka zote. Wakamkanusha, yakatokea kwao yaliyo tokea! Na imekuwa hikima ya Mwenyezi Mungu kuwa asiwakubalie hayo waliyo yataka, kwa kuchelea wasiikatae miujiza, kwa kutarajia watakuja amini miongoni mwao, au watakuja zaa watakao amini. Na miujiza hakika Sisi huwapeleka watu kwa kuwatia khofu na kitisho.

60 Ewe Nabii! Kumbuka tulipo kwambia: Hakika Mola wako Mlezi amewazunguka hao watu. Wao wamo wamedhibitiwa na kudra yake. Basi wewe wafikishie Ujumbe wala usimwogope yeyote katika wao. Mwenyezi Mungu atakulinda nao. Na mambo ya ajabu uliyo yaona katika Usiku wa Israi (Safari ya Usiku), hatukuyafanya Sisi ila yawe ni mtihani na majaribio kwa wanaadamu. Kwa hayo ipate kuzidi

- 61.** Na pale tulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam. Wakamsujudia isipo kuwa Iblisi. Akasema: Je! Nimsujudie uliye muumba kwa udongo?⁶¹
- 62.** Akasema: Hebu nambie khabari ya huyu uliye mtukuza juu yangu. Ukiniakhirisha mpaka Siku ya Kiyama, hapana shaka nitawaangamiza dhuriya zake wasipo kuwa wachache tu.⁶²
- 63.** Akasema Mwenyezi Mungu: Ondokelea mbali! Atakaye kufuata katika wao, basi Jahannamu itakuwa ndiyo malipo yenu, malipo ya kutimia.⁶³
- 64.** Na wachochee uwawezao katika wao kwa sauti yako, na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na waendao kwa miguu. Na shirikiana nao katika mali na wana, na waahidi. Na Shet'ani hawapi ahadi ila ya udanganyifu.⁶⁴
- 65.** Hakika wewe huna mamlaka juu ya waja wangu. Na Mola wako Mlezi anatosha kuwa ni wa kutegemewa.⁶⁵
- 66.** Mola wenu Mlezi ndiye anaye kuendesheeni marikebu katika bahari ili mtafute katika fadhila zake. Hakika Yeye ni Mwenye kukurehemuni nyinyi.⁶⁶
- 67.** Na inapo kufikieni taabu katika bahari, hao mnao waomba wanapotea, isipo kuwa Yeye tu. Na anapo kuvueni mkafika nchi kavu, mnageuka. Ama mwanaadamu ni mwingi wa kukanusha.⁶⁷
- 68.** Je! Mmeaminisha ya kuwa hataku didimizeni upande wowote katika nchi kavu, au kwamba hatakuleteeni tufani la kokoto? Kisha msipate wa kumtegemea.⁶⁸

Imani ya Muumini, na ukafiri wa kafiri. Na wala hatukuufanya ule mti ulio subiwa katika Qur'ani, nao ni Mti wa Zaquum, unao mea huko Motoni, isipo kuwa ni kuwafanyia wao pia mthani pale walipo sema: Moto unaunguza mti, basi vipi mti umee katika moto? Pia ni kuzidi kuwahadharisha kwa hayo. Lakini kuwahadharisha kwetu hakuwazidishii isipo kuwa kupindukia kiwango kikubwa kabisa.

61 Na Mwenyezi Mungu anakumbusha asli ya kuumba na uadui baina ya mwanaadamu na Iblisi, pale alipo waambia Malaika: Msujudieni Adam kwa kumuamkia na kumhishimu kwa kumuinamia. Hapo hapo wakasujudia. Isipo kuwa Iblisi akakataa, na akasema kwa chuki: Vipi nimsujudie uliye muumba kwa udongo, na hali mimi umeniumba kwa moto. Mimi ni bora kuliko yeye.

62 Iblisi akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Hebu nambie khabari za huyu uliye mtukuza juu yangu, ukaniamrisha nimsujudie. Kwa nini ukamtukuza kuliko mimi, na mimi ni bora kuliko yeye? Naapa kwa Utukufu wako! Ukinibakisha nihai mpaka Siku ya Kiyama, basi nitawahiliki dhuriya zao watao wazaa kwa kuwaghuri, isipo kuwa wachache tu kati yao utakao walinda na kuwahifadhi.

63 Mola akamwambia kwa kumtisha na kumlegezea kamba: Endelea na shani yako uliyo jichagulia kuifuata. Atakaye kut'ii wewe katika wana wa Adam, basi Jahannamu itakuwa ndiyo malipo yako na yao, malipo ya kutosha yaliyo kamilika.

64 Na wazuge na wavute kwa kuwaita wamuasi Mwenyezi Mungu hao unao waweza miongoni mwao. Na fanya kila juhudi yako ya namna zote za udanganyifu. Na shirikiana nao katika kuchuma mali ya haramu, na kuyatumia kwa haramu, na kuwakufurisha watoto na kuwaghuri wafanye fisadi. Na wape ahadi za uwongo, kama kuwa miungu yao itawaombea, na kuwa watapata utukufu kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya nasaba zao. Na Shetani hawaahidi wafwasi wake ila kwa udanganyifu na uficho.

65 Ama waja wangu walio nisafia niya Mimi wewe huna uwezo wa kuwapotoa, kwa kuwa wao wanamtegemea Mola wao Mlezi. Na Yeye anatosha kabisa kuwa ni wa kuwanusuru wakimtaka msaada wa kusalimika nawe.

66 Mola wenu Mlezi ni Yeye peke yake ndiye anaye ziendesha marikebu baharini ambazo kwazo nyinyi mnatafutia manufaa kwa biashara na mengineyo. Yeye daima ni Mwenye rehema kwenu.

67 Mkisibiwa na madhara na mkakabiliwa na khatari katika bahari, hukukimbieni wote hao muwaombao kwa haja zenu isipo kuwa Mwenyezi Mungu peke yake. Kwani nyinyi hapo hamumkumbuki mwenginewe. Lakini akisha kuvueni na kuzama na akakufikisheni nchi kavu, mnaacha Tawhid, kumuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja, na mnakufuru neema. Ndio mtindo wa binaadamu daima kukataa neema.

68 Na hapo tukisha kuvueni mkafika nchi kavu, kwani ndio mmeaminisha kuwa basi haikupateni adhabu ya Mwenyezi Mungu? Hasha! Akitaka anaweza akaipindua ardhi ikakuteketezeni chini yake. Na akitaka

69. Au mmeaminisha ya kuwa hatakurudisheni humo mara nyengine na kukupelekeeni kimbunga cha upepo akakuzamisheni kwa mlivyo kufuru, na kisha msipate wa kukunusuruni nasi.⁶⁹

70. Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba.⁷⁰

71. Siku tutapo waita kila kikundi cha watu kwa mujibu wa wakifuatacho - basi atakaye pewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, basi hao watasoma kitabu chao wala hawatadhulumiwa hata chembe.⁷¹

72. Na aliye kuwa hapa kipofu, basi atakuwa kipofu Akhera, na atakuwa aliye ipotea zaidi Njia.⁷²

73. Na hakika walikaribia kukushawishi uache tuliyo kufunulia ili utuzulie mengineyo. Na hapo ndio wangeli kufanya rafiki.⁷³

74. Na lau kuwa hatukukuweka imara ungeli karibia kuwaelekea kidogo.⁷⁴

75. Hapo basi bila ya shaka tungeli kuonjesha adhabu mardufu ya uhai, na adhabu mardufu ya kifo. Kisha usinge pata mtu wa kukunusuru nasi.⁷⁵

76. Na walitaka kukukera ili uitoke nchi. Na hapo wao wasingeli bakia humo ila kwa muda mchache tu.⁷⁶

atakupelekeeni upepo mkali ukutupieni kokoto na mawe, na wala msipate wa kukulindeni na yanayo kupatani.

69 Au nyinyi mmeaminisha kuwa Mola wenu Mlezi hatakurejesheni tena baharini, na akuleteeni tufani la upepo livunjilie mbali hicho chombo chenu? Akakuzamisheni kwa sababu ya kuto thamini neema yake pale alipo kuokoeni mara ya kwanza? Tena hapo hamtapata wa kukuteteeni kwetu kwa tuliyo kufanyieni ili mpate kusalimika.

70 Na hakika Sisi tumewatukuza wana wa Adam kwa kuwapa umbo zuri lilio nyooka, na matamshi, na uwezo wa kukhiari mambo. Na tukawapa hishima na utukufu pindi wakit'ii. Na tukawapakia nchi kavu juu ya wanyama, na baharini katika marikebu, na tukawaruzuku vitu vitamu, na tukawafadhilisha fadhila kubwa kuliko viumbe vingi kwa kuwapa akili na kuweza kufikiri.

71 Ewe Nabii! Waambie watu wako: Siku tutapo waita kila kikundi kwa alama zao wanazo zijua, au mwongozi wao wanaye mfuata, au Nabii, au Kitabu wakaambiwa: Enyi watu wa Musa! Au Enyi watu wa Qur'ani! Na kadhaalika, ili wapokee vitabu vya a'mali zao. Basi atakaye pokea kitabu cha a'mali zake kwa mkono wake wa kulia, na hao ndio wenye bahati njema, hao watasoma kitabu chao kwa furaha. Na wala hawatapunguziwa katika ujira wao duni ya kitu.

72 Ama yule wa kikundi kingine yatamhuzunisha atayo yaona. Na atazibiwa njia za kuokoka. Na atakuwa kipofu asione pa kuepuka adhabu yake, kama alivyo kuwa duniani kipofu haioni Njia ya Haki na Uwongofu! Na anaye kuwa duniani kipofu (wa moyo) basi Akhera ni kipofu zaidi, na yu mbali zaidi na Njia ya Kheri.

73 Hakika washirikina wanatafuta kila njia wakuachishe Qur'ani utafute miujiza myengineyo, ili uwe kama uliye tuzulia Sisi uwongo. Na hapo ndio watakuafanya uwe rafiki yao! Na hila hizi zimekaririwa na zimekuwa nyingi. Na kwa hivyo ungeli karibia kuyafuata wayatakayo, ila kwa kuwa wewe ni Mtume wetu uliye muaminifu, hayakuwa hayo.

74 Upole wetu umekugubika wewe, tukakulinda usiwakubalie matakwa yao, na tukakupa nguvu usimame juu ya Haki. Na lau kuwa si hayo ungeli karibia kuwakubalia kwa tamaa ya kuwa huenda ikafika siku imani yao ikakamilika baadae wakisha anza kuingia katika Uislamu.

75 Na lau ungeli karibia kuwaelekea hao, basi tungeli kukusanyia adhabu za duniani tukazifanya mardufu, na adhabu za Akhera nazo tukaziongeza mara mbili vile vile. Na wala usingeli pata yeyote wa kukunusuru na adhabu. Lakini hayo hayawi kabisa, hayawezi kumfikilia Mtume wetu Muaminifu.

76 Na makafiri wa Makka wamejaribu, na walikaribia kukuudhi mpaka wakutoe kwenye ardhi ya Makka kwa uadui wao na chuki zao. Na lau yangeli kuwa hayo, basi wao nao wasingeli baki humo ila muda mchache tu, kisha washindwe katika hayo mambo yao, na hukumu iwe ya Mwenyezi Mungu.

77. Huo ndio mwendo kwa Mitume tulio watuma kabla yako. Wala hupati mabadiliko katika mwendo wetu.⁷⁷
78. Shika Sala jua linapo pinduka mpaka giza la usiku, na Qur'ani ya al fajiri. Hakika Qur'ani ya alfajiri inashuhudiwa daima.⁷⁸
79. Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunna khasa kwako wewe. Huenda Mola wako Mlezi akakunyanyua cheo kinacho sifika.⁷⁹
80. Na sema: Mola wangu Mlezi! Niingize muingizo mwema, na unitoe kutoka kwema. Na unipe nguvu zinazo toka kwako zinisaidie.⁸⁰
81. Na sema: Kweli imefika, na uwongo umetoweka. Hakika uwongo lazima utoweke!⁸¹
82. Na tunateremsha katika Qur'ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila khasara.⁸²
83. Na mwanaadamu tunapo mneemesha hugeuka na kujitenga kando. Na inapo mgusa shari hukata tamaa.⁸³
84. Sema: Kila mmoja anafanya kwa nama yake. Na Mola wenu Mlezi anajua aliye ongoka katika njia.⁸⁴
85. Na wanakuuliza khabari za Roho. Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi. Nanyi hamkupewa katika ilimu ila kidogo tu.⁸⁵
86. Na tungeli penda tungeli yaondoa tuliyo kufunulia. Kisha usingeli pata mwakilishi wa kukupigania kwetu kwa haya.⁸⁶

77 Na huo ndio mwendo wetu kwa Mitume wa kabla yako - huwahiliki wale wanao wafukuza Manabii wao. Na wala hapana mabadiliko katika mwendo wetu.

78 Shika Sala zilizo faridhiwa, tangu kupinduka jua kati ya mbingu kuelekea upande wa machwea jua, mpaka kiza cha usiku. Na hizi ndizo Sala za Adhuhuri, Alasiri, Magharibi na Isha. Na pia shika Sala ya Alfajiri ambayo wanaishuhudia Malaika.

79 Na katika wakati wa usiku amka, kwa kusali Sala ya Tahajjud. Hiyo ni ibada ya zaidi juu ya zile Sala Tano. Hii imekukhusu wewe tu, kwa kutaraji kuwa Mola wako Mlezi atakuweka Siku ya Kiyama makamo watakao kusifia viumbe.

80 Na sema: Ewe Mola Mlezi! Niingize maingizo ya kuridhisha matukufu katika kila unapo niingiza katika jambo au pahala. Na unitoe kwa kutoka kunako ridhisha kutukufu. Na kwa fadhila yako nijaalie nguvu za kunisaidia niwashinde maadui zangu.

81 Na sema ukiaonya watu wako washirikina: Haki ya Tawhid, Imani ya Mungu Mmoja, na Dini ya Kweli na Uadilifu, imekwisha fika. Na uwongo, na ushirikina, na dini ya ufisadi na dhulma, yote hayo yameondoka. Kwani uwongo daima hauna dawamu.

82 Na vipi Haki isiwe na nguvu na hali Sisi tunateremsha katika Qur'ani dawa ya kuponyesha maradhi ya shaka katika vifua vya watu, na sababu za kuwapatia rehema wanao iamini! Na madhaalimu hawana linao wazidia ila khasara tu kwa kuikataa kwao.

83 Na hakika katika maumbile ya mwanaadamu ni kujidanganya na kukata tamaa. Tukimneemesha kwa kumpa uzima na ukunjufu wa mali, hupuuza kutukumbuka na kutuomba, na hujitenga nasi kwa kiburi na majivuno! Na akiguswa na shari, kama ugonjwa na ufakiri, huwa mwingi wa kukata tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu.

84 Ewe Nabii! Waambie makafiri wa Kikureshi kwa kuepuka kuchochea ugomvi na makindano: Kila mmoja wetu na mmoja wenu anatenda na anakwenda kwa kufuata njia yake. Na Mola wenu Mlezi ni Mjuzi mno, wala hana ajuaye kuliko Yeye kumjua nani aliye shika njia sawa na kufuata Haki. Na huyo humlipa ujira wake kaamili. Na kumjua aliye potea njia, na huyo humpa adhabu kama anayo stahiki.

85 Ewe Muhammad! Watu wako wanakuuliza kwa kutomezwa na Mayahudi: Nini hakika ya Roho? Waambie: Roho ni katika ilimu yake Mwenyewe Mola wangu Mlezi aliyo jikhusisha nayo Yeye. Na nyinyi hamkupewa ilimu ila chache tu ukilinganisha na ilimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

86 Na lau tungeli taka kuifuta kabisa kifua hiyo Qur'ani tuliyo kufunulia tungeli fanya hivyo, na kisha usingeli mpatia yeyote wa kukunusuru katika watu wako.

87. Isipo kuwa iwe rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi. Hakika fadhila yake kwako ni kubwa.⁸⁷
88. Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao.⁸⁸
89. Na hakika tumewaeleza watu katika hii Qur'ani kwa kila mfano. Lakini watu wengi wanakataa isipo kuwa kukanusha tu.⁸⁹
90. Na walisema: Hatutakuamini mpaka ututimbulie chemchem katika ardhi hii.⁹⁰
91. Au uwe na kitalu cha mitende na mizabibu, na utupitishie mito kati yake ikimiminika.⁹¹
92. Au utuangushie mbingu vipande vipande kama ulivyo dai; au utuletee Mwenyezi Mungu na Malaika uso kwa uso.⁹²
93. Au uwe na nyumba ya dhahabu, au upae mbinguni. Wala hatutaamini kupaa kwako mpaka ututeremshie kitabu tukisome. Sema: *Subhana Rabbi*, Ametakasika Mola wangu Mlezi! Kwani mimi ni nani isipo kuwa ni mwanaadamu na Mtume?⁹³
94. Na nini kilicho wazuilia watu kuamini ulipo wajia uwongofu isipo kuwa walisema: Je! Mwenyezi Mungu humtuma mwanaadamu kuwa ni Mtume?⁹⁴
95. Sema: Ingeli kuwa duniani wapo Malaika wanatembea kwa utulivu wao, basi bila ya shaka tungeli wateremshia Malaika kuwa ni Mtume wao.⁹⁵
96. Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi baina yangu na nyinyi. Hakika Yeye anawajua vyema waja wake na anawaona.⁹⁶

87 Lakini tumeiacha Qur'ani ibaki vile vile kifuani mwako kwa rehema kutoka kwa Mola wako Mlezi, kwani fadhila zake kwako wewe ni kubwa mno katika muujiza huu.

88 Waambie, kwa kushindana nao, kama wanaweza walete mfano wake. Nao hawawezi! Hata wakikusanyika watu na majini wakasaidiana kuleta mfano wa hii Qur'ani kwa mpango wake na maana yake, hawawezi; na wanga saidiana wao kwa wao.

89 Na katika Qur'ani hii tumewaeleza watu kwa namna mbali mbali kila maana kama ni mifano katika maajabu yake. Lakini watu wengi walikataa ila kupinga na kuchukia.

90 Ilipo dhihiri kushindwa kwao na Qur'ani, na wakabanwa kwa hoja, wakataka waletewe ishara nyingine na miujiza mingine. Hicho ni kitendo cha mwenye kushindwa hoja, aliye emewa na kutahayari. Ndio wakasema: Hatutokuamini mpaka ututimbulie katika ardhi ya Makka chemchem ambayo maji yake hayakatiki.

91 Au uwe nacho kitalu Makka cha mitende na mizabibu chenye kupita mito kati yake! (Kwa kujua kuwa ardhi ya Makka ni kavu haioti kitu.)

92 Au mbingu ituangukie vichwani mwetu kwa mapande kama ulivyo dai kuwa Mwenyezi Mungu anatauhidi hayo. Au utuletee Mwenyezi Mungu na Malaika tukabiliane nao macho kwa macho!

93 Au uwe na nyumba iliyo pambwa kwa dhahabu, au upae mbinguni. Na hata hivyo hatukusadiki mpaka ukituletea kitabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kinacho thibitisha ukweli wako tukisome! Waambie: Mola wangu Mlezi ametakasika kabisa na kuhukumiwa na yeyote, au yeyote kushirikiana naye katika kudra yake! Mimi si chochote ila ni mwanaadamu kama Mitume wote wengineo. Na wala wao hawakuwaleta watu wao muujiza ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

94 Na nini kilicho wazuilia washirikina wa Makka kuifuata Haki ulipo wajia wahyi (ufunuo) pamoja na miujiza isipo kuwa madai yao kwa ujinga wao ya kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hatumi Mitume wanaadamu, ila huwa ni Malaika!

95 Sema kwa kuwarudi: Lau kuwa duniani badala ya wanaadamu wapo Malaika wanatembea kama wanaadamu na wamekaa humo, basi tungeli wateremshia kutoka mbinguni Malaika kuwa ni Mitume wao katika jinsi yao. Lakini Malaika si kama binaadamu; na wangeli kuja basi wange kuja kwa sura za watu.

96 Sema: Kama mnaukataa Utume wangu, basi Mwenyezi Mungu anatosha kuwa ni wa kutuhukumu baina yangu na nyinyi, akathibitisha ukweli wa Ujumbe wangu kwenu. Hakika Yeye kwa waja wake ni Mwenye kujua hali zenu, na Mwenye kuviona vitendo vyenu. Naye ni Mwenye kukulipeni kwa hivyo.

97. Na anaye mhidi Mwenyezi Mungu basi huyo ndiye aliye hidika. Na anaye wapotoa basi huto wapatia walinzi badala yake. Na tutawakusanya Siku ya Kiyama hali wakikokotwa juu ya nyuso zao, nao ni vipofu na mabubu na viziwi. Na makaazi yao ni Jahannamu. Kila moto ukifanya kusinzia tutazidi kuuchochea uwake kwa nguvu.⁹⁷

98. Hayo ni malipo yao kwa sababu walizikataa ishara zetu, na wakasema: Hivyo tukisha kuwa mifupa na mapande yaliyo vurugika tutafufuliwa kwa umbo jipya?⁹⁸

99. Kwani hawakuona ya kwamba Mwenyezi Mungu aliye umbu mbingu na ardhi ni Mwenye kuweza kuumba mfano wao? Na Yeye amewawekea muda usio na shaka yoyote. Lakini madhaalimu hawataki ila ukafiri.⁹⁹

100. Sema: Lau kuwa nyinyi mnazimiliki khazina za rehema za Mola wangu Mlezi, basi hapana shaka mngeli zuia kuzitumia kwa ajili ya kukhofu. Na mwanaadamu tangu hapo tabia yake ni mchoyo!¹⁰⁰

101. Na kwa yakini tulimpa Musa ishara tisa zilizo wazi. Waulize Wana wa Israili alipo wafikia, na Firauni akawaambia: Hakika mimi nakuona wewe Musa umerogwa!¹⁰¹

102. Musa akasema: Wewe unajua bila ya shaka kuwa haya hakuyateremsha ila Mola Mlezi wa mbingu na ardhi ili kuwa ni ushahidi wa kuonekana. Na hakika mimi bila ya shaka nakuona wewe, Firauni, kuwa umekwisha angamia.¹⁰²

103. Basi Firauni akataka kuwafukuza katika nchi. Kwa hivyo tukamzamisha yeye na walio kuwa pamoja naye wote.¹⁰³

104. Na tukawaambia baada yake Wana wa Israili: Kaeni katika nchi. Itapo kuja ahadi ya Akhera tutakuleteni nyote pamoja.¹⁰⁴

97 Waambie: Yule ambaye Mwenyezi Mungu anamwongoa kwa kuwa yu tayari kufuata uwongofu, basi huyo ni mwongofu. Na anaye mpotoa kwa kufisidika khulka yake, hutopata wa kuwanusuru asiye kuwa Yeye wa kuwaongoa duniani. Na Akhera tutawakusanya wakikokotwa juu ya nyuso zao, hawaoni, wala hawasemi, wala hawasikii. Na mahali pao wanapo pelekwa kukaa ni Jahannamu. Kila moto ukipungua ukali wake Mwenyezi Mungu anazidi kuuchochea uwake kwa nguvu zaidi.

98 Adhabu hiyo ndiyo malipo yao kwa sababu ya kuzikataa dalili tulizo waletea za kuthibitisha Haki, na kwa ile kauli yao kusema: Hivyo sisi tutafufuliwa kwa umbo jipya baada ya kwisha kuwa mifupa na vumbi?

99 Jee wameghafilika na hawakujua kwamba Mwenyezi Mungu aliye umbu mbingu na ardhi, juu ya ukubwa wao, ni Mwenye kuweza kuumba watu na majini kama wao? Na Mwenye kuweza hayo, vipi awe hawezi kuwarejesha wao upya, na hilo ni jepesi zaidi kwake! Na Yeye *Subhanahu* ameweka muda maalumu wa kuwarejesha tena baada ya kwisha kufa, na huo hauna shaka kuwa. Na muda huo ndio Siku ya Kiyama. Na juu ya hivyo walio zidhulumu nafsi zao kwa ukafiri wanakataa baada ya kuletewa hoja hizi. Na hayo si kwa lolote ila kwa ukafiri tu.

100 Waambie hawa washirikina: Lau kuwa mnazimiliki riziki za Mola wangu Mlezi, mngeli zifanyia ubakhili kwa kuogopa ufakiri. Kwani ni tabia ya watu kuwa na pupa na ubakhili. Na Mwenyezi Mungu, Mkwasi na Karimu, humpa anacho taka amtakaye, na huteremsha miujiza aitakayo Yeye, sio waitakayo watu. Na Yeye katika yote hayo ni Mwenye hikima na Mjuzi.

101 Na lau hawa watu wangeli letewa hizo ishara wazitakazo, wange zigeuzia uso, wala wasinge ziamini! Na Sisi tulimpa Musa Ishara tisa wazi (1). Na juu ya hivyo wakakufuru. Na Firauni akasema: Hakika mimi nakuona wewe, Musa, ni mtu uliye rogwa! (*Tazama Maelezo 17:101*)

102 Musa akasema: Ewe Firauni! Unajua vyema kuwa aliye ziteremsha Ishara hizi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi. Kwani ni Yeye ndiye Mwenye kuweza hayo. Nazo Ishara hizo zi wazi, zinakuonyesha ukweli wangu. Lakini wewe unafanya kiburi na inadi tu. Na hakika mimi nakuona wewe, Firauni, kuwa ni mwenye kuangamia ikiwa hutoacha inadi yako.

103 Firauni akashikilia uasi wake, akataka kumtoa Musa na Wana wa Israili katika nchi ya Misri. Tukamzamisha yeye na askari wake wote.

104 Tukamvua Musa na kaumu yake, na baada ya kumzamisha Firauni tukasema kuwaambia Wana wa

105. Na kwa Haki tumeiteremsha, na kwa Haki imeteremka. Na hatukukutuma ila uwe mbashiri na mwonyaji.¹⁰⁵
106. Na Qur'ani tumeigawanya sehemu mbali mbali ili uwasomee watu kwa kituo, na tumeiteremsha kidogo kidogo.¹⁰⁶
107. Sema: Iaminini au msiiamini. Hakika wale walio pewa ilimu kabla yake, wanapo somewa hii, huanguka kifudifudi wanasujudu.¹⁰⁷
108. Na wanasema: *Subhana Rabbina*, Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika ahadi ya Mola wetu Mlezi lazima itimizwe!¹⁰⁸
109. Na huanguka kifudifudi na huku wanalia, na inawazidisha unyenyekevu.¹⁰⁹
110. Sema: Mwombeni *Allah* (Mwenyezi Mungu), au mwombeni *Rahman* (Mwingi wa Rehema), kwa jina lolote mnalo mwita. Kwani Yeye ana majina mazuri mazuri. Wala usitangaze Sala yako kwa sauti kubwa, wala usiifiche kwa sauti ndogo, bali shika njia ya kati na kati ya hizo.¹¹⁰
111. Na sema: *Alhamdulillah*, Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye hana mwana, wala hana mshirika katika ufalme, wala hana rafiki wa kumsaidia kwa sababu ya udhaifu wake. Na mtukuze kwa utukufu mkubwa.¹¹¹

Israili: Kaeni katika nchi takatifu ilioko Sham. Ukija wakati wa uhai wa pili tutakutoeni makaburini kwenu kwa mchanganyiko. Kisha tutakuhukumuni kwa uadilifu.

105 Na hatukuiteremsha Qur'ani ila kwa kuunga mkono hikima ya Mwenyezi Muungu, iliyo pelekea kuteremshwa kwake. Nayo hiyo Qur'ani kwa dhati yake haikuteremka ila kuwa imekusanya Ukweli wote. Kwani itikadi zake ndizo zilizo sawa, na hukumu zake ndizo zilizo nyooka. Na wewe, ewe Nabii, hatukukutuma ila uwe mbashiri wa kuwabashiria Pepo wenye kuamini, na mwonyaji kuwaonya wanao ukanya Moto. Basi wewe huna jukumu lolote ikiwa wao hawaamini.

106 Na hii Qur'ani tumeigawa na tumeiteremsha kipande kipande kwa muda mrefu, ili uwasomee watu kwa taratibu wapate kuifahamu. Tumeiteremsha kidogo kidogo kwa utulivu bila ya matatanisho.

107 Waambie makafiri wa Makka kwa kuwatisha: Jichagulieni nafsi zenu mlitakalo - kuiamini Qur'ani au la! Kwani hakika walio pewa ilimu sawa na fahamu baraabara kabla ya kuteremka kwake, wakismewa Qur'ani huangukia kwenye nyuso zao kwa kusujudu na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu.

108 Na wao husema: Mola wetu Mlezi ametakasika na ila ya kwenda kinyume na ahadi yake ya kuneemesha na kuadhibu alio ahidi. Kwani ahadi yake lazima itimie bila ya shaka yoyote.

109 Na huangukia tena kwenye nyuso zao mara ya pili wakilia kwa kumkhofu Mwenyezi Mungu, na Qur'ani inawazidisha unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu.

110 Waambie hawa washirikina: Mwiteni Mwenyezi Mungu kwa jina la *Allah*, au jina la *Rahman*; kwani jina lolote mtalo mwitia ni zuri. Yeye Mtukufu ana majina mengi mazuri mazuri. Wala hamdanganyikiwi kwa kutumia majina mengi kuwa kwa hivyo mwenye kuitwa ni zaidi ya Mmoja. Na unapo soma Qur'ani katika Sala zako, basi usipaze sauti yako wakasikia washirikina wakakusibabi na wakakuudhi. Wala usifanye kwa siri hata Waumini wakawa hawasikii. Kuwa kati kati katika kusoma kwa.

111 Nasema *Alhamdulillah*, Himdi zote, yaani sifa na shukrani, ni za Mwenyezi Mungu ambaye hakuzaa mwana, kwani hamhitajii; wala hana mshirika katika ufalme, kwani Yeye peke yake ndiye aliye uanzisha; wala hana msaidizi wa kumtia nguvu kwa udhaifu fulani unao mpata. Na mtukuze Mola wako Mlezi kwa utukufu mkubwa ulio laiki naye.

Sura 18 - Al-Kahf

Utangulizi

Sura hii ni ya Makka, isipo kuwa Aya 38, na Aya zinazo anzia 83 mpaka 101. Basi zimo Aya ishirini za Madina. Nayo imeanzia kwa kumhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuiteramsha Qur'ani Tukufu, na kubainisha kuwa Qur'ani ni onyo na bishara. Ndani yake lipo onyo kwa wanao dai kuwa ati Mwenyezi Mungu ana mwana. Na humu imetajwa hamu kubwa aliyo nayo Nabii ya kutaka waamini wale anao waita kwenye mlingano wa Mwenyezi Mungu. Kisha kikatajwa kisa cha Ahlil Kahf, Watu wa Pangoni, walio lala usingizi kisha wakaamka baada ya kukaa katika pango lao muda wa miaka mia tatu na tena wakazidishiwa tisa. Na watu hao walikuwa Wakristo walio kuwa wakikimbia udhalimu wa mtawala wa Kirumi. Wakalala katika pango muda huo, kisha wakaamka ili kuwa ni ishara ya uweza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kufufua baada ya kufa.

Kisha baada ya hayo Mwenyezi Mungu akamuamrisha kusoma Qur'ani na aitumie kwa kuonya na kubashiri. Kisha imebainishwa hali ya watu wa Peponi na watu wa Motoni. Na Mwenyezi Mungu akapiga mifano ya watu wawili, mmoja tajiri anajitapa kwa mali yake na wanawe. Na wa pili anatafakhari kwa Mwenyezi Mungu wake. Na amebainisha *Subhanahu* kuwa ulinzi wake ndio wa Haki. Na tena *Subhanahu* ameeleza starehe ya duniani inayo pita, na neema ya daima au adhabu chungu ya Siku ya Kiyama. Tena *Subhanahu* ametaja hadithi ya Musa pamoja na Mja Mwema aliye pewa ilimu kutokana na Mwenyezi Mungu. Na katika kisa hichi inapatikana sura ya vipi mtu anaweza asijue mambo, hata akiwa Nabii Mtume katika Mitume imara - Ulul a'zmi - kwa kudra yake Mwenyezi Mungu, ila akiwa Yeye Mwenyezi Mungu akimjuulisha. Tena anatajwa Dhul-qarnaini na kufika kwake mashariki ya mbali, na alivyo jenga Ukuta. Kisha yatakayo kuwa Siku ya Kiyama, na malipo ya Waumini, na ilimu ya Mwenyezi Mungu na maneno yake yasiyo malizika. Na Sura ikakhitimishia kwa kueleza Njia ya Kumridhi *Subhanahu*.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

1. Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, ambaye amemteremshia mja wake Kitabu, wala hakukifanya kina upogo.¹
2. Kimenyooka sawa, ili kitoe onyo kali kutoka kwake, na kiwabashirie Waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri.²

1 Kuhimidiwa, yaani kusifiwa na kushukuriwa kwa wema, anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye amemteremshia mja wake, Muhammad, hii Qur'ani. Na wala hakujaalia kuwa ndani yake kipo chochote cha dosari, kilicho kwenda kombo na kuacha usawa. Bali ndani yake mna Haki tupu, isiyo na shaka yoyote.

2 Na Mwenyezi Mungu ameijaalia Qur'ani imesimama, imenyooka sawa sawa katika mafunzo yake ili kuwaonya wanao kufuru na kukataa, kuwa watapata adhabu kali itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na iwape bishara njema wanao isadiki, ambao wanatenda vitendo vyema, ya kwamba watapata malipo mazuri.

3. Wakae humo milele.³
4. Na kiwaonye wanao nena: Mwenyezi Mungu ana mwana.⁴
5. Wao hawana ujuzi wa jambo hili, wala baba zao. Ni neno kuu hilo litokalo vinywani mwao. Hawasemi ila uwongo tu.⁵
6. Huenda ukajihiliki nafsi yako kwa ajili yao, kuwasikitikia kwa kuwa hawayaamini mazungumzo haya!⁶
7. Kwa hakika tumevifanya vilioko juu ya ardhi kuwa ni pambo lake ili tuwafanyie mtihani, ni nani kati yao wenye vitendo vizuri zaidi.⁷
8. Na hakika Sisi tutavifanya vyote vilio juu ya ardhi kuwa kama nchi ilio pigwa na ukame.⁸
9. Bali unadhani ya kwamba wale Watu wa Pangoni na Maandishi walikuwa ni ajabu miongoni mwa ishara zetu?⁹
10. Vijana hao walipo kimbilia kwenye pango walisema: Mola wetu Mlezi! Tupe rehema itokayo kwako, na tutengezee uwongofu katika jambo letu.¹⁰
11. Tukayaziba masikio yao kuwalaza humo pangoni kwa muda wa miaka kadhaa wa kadhaa.¹¹
12. Kisha tukawazindua ili tujue ni lipi katika makundi mawili lilio hisabu sawa muda walio kaa.¹²
13. Sisi tunakusimulia khabari zao kwa kweli. Hakika wao walikuwa ni vijana walio muamini Mola wao Mlezi. Na Sisi tukawazidisha uwongofu.¹³

3 Malipo hayo ni Pepo watakayo kaa humo milele.

4 Na kiwaonye kwa njia makhsusi wale walio msingizia Mwenyezi Mungu kuwa ana mwana, na hali Yeye ametakasika kuwa kama viumbe, akawa mwenye kuzaa au akazaliwa mtoto wake.

5 Wala wao hawana ujuzi wowote wa hayo wala baba zao hawakuwa nao huo. Ni uzushi mkubwa mno huu wa kutoa neno hili vinywani mwao! Wayasemayo ni uzushi, na wala hapana uzushi mkubwa kushinda huu.

6 Ewe Nabii! Usijihiliki nafsi yako bure kwa kuhuzunika na kusikitika kwa kuacha kwao kuitikia Wito wako, na kuisadiki hii Qur'ani.

7 Sisi tumewaumba kwa kheri na shari, na tumevifanya vilio juu ya ardhi ni pambo lake kwa ajili ya manufaa ya watu wake. Hivyo tunawatendea vitendo kama ni mtihani wapate kudhihiri kati yao wenye a'mali njema. Basi aliye pumbazwa na ulimwengu, na asiishughulikie Akhera, huwa amepotea. Na aliye iamini Akhera, huyo huwa ameongoka.

8 Baada ya kumalizika dunia Sisi tutavifanya vyote vilio juu ya dunia kama ardhi tambarare isio na mimea baada ya kuwa imeamirika kwa mazao ya kijani yenye uhai.

9 Walio pumbazwa na starehe za dunia wanakanya kufufuliwa, ilihali hakika ya mambo inathibitisha pana uhai baada ya usingizi mrefu. Na hichi kisa cha Watu wa Pangoni kwenye mlima na bao lilio andikwa majina yao baada ya kufa kwao hakikuwa ni ajabu ya pekee, tukaziacha ishara zote nyenginezo. Ijapo kuwa kisa hicho si cha kawaida, lakini hakikuwa ndio cha ajabu kushinda ishara zetu nyengine zenya kuonyesha uweza wetu.

10 Taja pale walipo kwenda hao vijana kwenye pango, wakafanya hapo ndipo pahali pa kujificha baada ya kukimbia ushirikina na washirikina kuhifadhi Dini yao. Wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Tupe maghfira kutoka kwako, na utulinde na adui yetu, na tusahilishie hidaya na tawfiki katika mambo yetu!

11 Tukaipokea dua yao hiyo, tukawalaza kwa salama katika hilo pango kwa muda wa miaka kadhaa wa kadhaa.

12 Kisha Mwenyezi Mungu aliwaamsha baada ya kulala kwa muda mrefu, ili matokeo yake yawe ni kudhihirisha ujuzi wetu ni nani katika makundi mawili aliye sibu kukisia muda wa kulala kwao.

13 Ewe Mtume! Sisi tunakusimulia khabari zao kwa kweli kweli: Hakika hao walikuwa vijana katika zama zilizo pita ambao walikuwa wameshika Dini ya Haki. Walimuamini Mola wao Mlezi kuwa ni Mmoja tu, na ilihali wamezungukwa na washirikina. Na Sisi tukawazidisha wawe na yakini.

14. Na tukazitia nguvu nyoyo zao walipo simama na wakasema: Mola wetu Mlezi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi. Hatutamwita mwenginewe kabisa badala yake kuwa ni Mungu. Hivyo itakuwa tumesema jambo la kuvuka mpaka.¹⁴

15. Hawa watu wetu wameshika miungu mingine badala yake Yeye. Kwa nini basi hawawatolei uthibitisho ulio dhaahiri? Na nani aliye dhaalimu zaidi kuliko anaye muzulia uwongo Mwenyezi Mungu?¹⁵

16. Na mkijitenga nao na vile wanavyo viabudu badala ya Mwenyezi Mungu, basi kimbilieni pangoni, akufungulieni Mola wenu Mlezi rehema yake, na akutengenezeeni ya kukufaeni katika mambo yenu.¹⁶

17. Na unaliona jua linapo chomoza linainamia kuliani mwao kutoka hapo pangoni; na linapo kuchwa linawakwepa kushotoni, na wao wamo katika uwazi wa pango. Hizo ni katika ishara za Mwenyezi Mungu. Ambaye Mwenyezi Mungu anamwongoa basi huyo ni mwenye kuongoka. Na anaye muacha kupotea basi hutampatia mlinzi wala mwongozi.¹⁷

18. Nawe utawadhandia wamacho, na hali wamelala. Nasi tunawageuza kulia na kushoto. Na mbwa wao amenyoosha miguu yake ya mbele kizingitini. Kama ungeli watokea hapana shaka ungeli geuka kuwakimbia, nawe umejaa khofu.¹⁸

19. Na kwa namna hii tuliwainua usingizini wapate kuulizana wao kwa wao. Alisema msemaji katika wao: Mmekaa muda gani? Wakasema: Tumekaa siku moja au sehemu ya siku. Wakasema: Mola wenu Mlezi anajua zaidi muda mlio kaa. Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi fedha zenu ende mjini, akatazame chakula chake kipi kilicho bora kabisa akuleteeni cha kukila. Naye afanye mambo hayo kwa busara, wala asikutajeni kabisa kwa yeyote.¹⁹

14 Na tulizithibitisha nyoyo zao juu ya Imani na subira ya kuvumilia shida, pale walipo simama mbele ya watu wao wakasema kwa kujifunga kwa ahadi: Ewe Mola wetu Mlezi! Wewe ndiye wa Haki, Mola Mlezi wa mbingu na ardhi! Sisi hatumuabudu mungu mwenginewe. Wala hatutoiwacha itikadi hii. Wallahi! Tukisema jenginelo basi itakuwa tunasema lilio mbali kabisa na kweli!

15 Kisha wakaambiana wenyewe kwa wenyewe: Hawa watu wetu wamemshirikisha Mwenyezi Mungu. Lau kuwa wameleta hoja iliyo wazi ya kuthibitisha ungu wa hivyo wanavyo viabudu badala ya Mwenyezi Mungu! Hakika watu hawa ni wenye kudhulumu kwa vitendo vyao hivyo. Wala hapana aliye zidi udhaalimu kuliko mwenye kumzulia Mwenyezi Mungu uwongo kwa kumsingizia washirika.

16 Na wakaambiana wao kwa wao: Maadamu sisi tumejitenga nao hao katika ukafiri wao na ushirikina wao, basi kimbilieni pangoni mlinde Dini yenu. Mola wenu Mlezi atakukunjulieni maghfira yake, na atakusahilishieni mambo yenu kwa njia za kukufaeni katika maisha yenu. (*Tazama Maelezo 18:16*)

17 Na lile pango lilikuwa kwenye mlima, lina nafasi ndani. Lिलielekea kaskazini, linapigwa na upepo mzuri. Jua likichomoza muanga wake huwa kuliani mwao, na miale yake huwa mbali nao; na likichwa huwa kushotoni mwao. Kwa hivyo lile jua halipigi ndani ya pango, na kwa hivyo walisalimika na joto la jua, na upepo wa kaskazi unawaingilia. Na yote hayo ni katika ishara za kudra ya Mwenyezi Mungu. Na anaye pata tawfiki ya Mwenyezi Mungu kuokoka basi huokoka, na aliye kosa tawfiki hatopata wa kumwongoa baada yake.

18 Na wewe ukiwaona utadhani wamacho, nao kwa hakika wamelala. Na katika usingizi wao tulikuwa tunawageuza kulia na kushoto mara kwa mara ili kuwahifadhi miili yao isidhurike na ardhi wakafanya madonda. Na mbwa aliye wafuata alinyoosha miguu yake ya mbele mlangoni, naye kalala pia kama kwamba yu macho. Ungeli watokea nao wamo katika hali ile ungeli toka mbio na moyo umejaa khofu kwa walivyo kuwa wanatisha katika kulala kwao. Hapana anaye waona ıla atashika nao. Hayo ili wasikaribiwe na mtu, wala wasiguswe na mtu mpaka wishe muda wao.

19 Kama tulivyo walaza tuliwaamsha wapate kuulizana wenyewe kwa wenyewe wamelala muda gani? Mmoja wao akasema: Umekupitieni muda gani katika usingizi? Wakasema: Tumelala muda wa siku au baadhi ya siku. Walivyo kuwa hawana yakini nayo hayo wakasema: Mwachieni mambo haya Mwenyezi

20. Kwani wao wakikutambueni watakupigeni mawe, au watakurudisheni katika dini yao; na hapo hamtafanikiwa kabisa!²⁰

21. Na namna hivi tuliwa juulisha kwa watu wapate kujua ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli, na kwamba Saa haina shaka. Walipo kuwa wakigombania jambo lao wao kwa wao walisema: Jengeni jengo juu yao. Mola wao Mlezi anawajua vyema. Wakasema walio shinda katika shauri yao: Bila ya shaka tutawajengea msikiti juu yao.²¹

22. Watasema: Walikuwa watatu, wa nne wao ni mbwa wao. Na wanasema: Walikuwa watano, wa sita wao ni mbwa wao. Wanavurumisha ovyo. Na wanasema: Walikuwa saba, na wa nane wao ni mbwa wao. Sema: Mola wangu Mlezi ndiye anaye jua sawa sawa hisabu yao. Hawawajui ila wachache tu. Basi usibishane juu yao ila kwa mabishano ya juu juu tu hivi. Wala usiulize khabari zao kwa yeyote yule.²²

23. Wala usisema kamwe kwa jambo lolote lile: Hakika nitalifanya hilo kesho-²³

24. Isipo kuwa Mwenyezi Mungu akipenda. Na mkumbuke Mola wako Mlezi pale unapo sahu, na sema: Asaa Mola wangu Mlezi ataniongoa kwenye uwongozi ulio karibu zaidi kuliko huu.²⁴

25. Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu, na wakazidisha tisa.²⁵

26. Sema: Mwenyezi Mungu anajua zaidi muda walio kaa. Ni zake tu siri za mbingu na ardhi. Kuona kulioje na kusikia kwake! Hawana mlinzi isipo kuwa Yeye, wala hamshirikishi yeyote katika hukumu yake.²⁶

Mungu; kwani Yeye ni Mjuzi zaidi wa haya. Na ende mmoja wenu mjini, na achukue hizi sarafu za fedha achague chakula kizuri kabisa akuleteeni mle. Na awe na mafahamiano mema. Wala mambo yenu yasijuulikane na mtu yeyote.

20 Kwani hao watu wakikuoneni watakuuweni kwa kukupopoeni mawe, au watakurejesheni katika ukafiri kwa nguvu. Nanyi mkirejea ukafirini basi hamtaongokewa kabisa duniani wala Akhera.

21 Na kama tulivyo walaza na tukawaamsha tulikuja watambulisha kwa watu wa ule mji wapate kujua kuwa ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kufufua wafu ni ya kweli. Na Kiyama hapana shaka kitakuja. Watu wa ule mji wakamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Kisha Mwenyezi Mungu akawafisha wale vijana. Watu sasa wakazozana kwa mintarafu yao. Baadhi yao wakasema: Jengeni jengo kwenye mlango wa pango, na tuwaache wao na shani yao. Kwani Mola wao Mlezi anajua vyema hali yao. Na wakasema wenye kusikilizwa miongoni mwao: Hapa pahala pao tutafanya msikiti kwa sababu ya ibada.

22 Watasema kikundi fulani katika Watu wa Kitabu (Biblia) wanao jiingiza katika mzozano wa kisa cha *Ahlil Kahf* (Watu wa Pangoni) kwamba hao walikuwa watatu na wa nne wao ni mbwa wao. Na wengine wanasema: Walikuwa watano, na wa sita wao ni mbwa wao. Tena wengine wanasema: Wao ni saba, na wa nane wao ni mbwa wao. Waambie hawa wanao khitalifiana: Mola wangu Mlezi ni Mjuzi ambaye hapana wa kumshinda ujuzi wake kuijua idadi yao. Wala hapana wajuao ila watu wachache tu ambao Mwenyezi Mungu amewajuvya hisabu yao. Basi wewe usijadiliane na hao wanao khitalifiana juu ya mas-ala ya hao vijana, ila majadiliano ya juu juu ya upole, bila ya kujaribu kuwakinaisha. Kwani wao hawakinaiki. Wala msimulize yeyote kati yao juu ya khabari zao. Wewe hakika imekwisha kujia iliyo kweli isiyo na shaka.

23 Wala usiseme kabisa kwa jambo unalo azimia kuliendea na kujihimu kulitenda: Mimi nitalifanya hilo baadae!

24 Ila kusema huko kuambatane na kupenda kwa Mwenyezi Mungu kwa kusema: Inshallah, yaani Mwenyezi Mungu akipenda. Na ukisahau jambo, basi kimbilia kumtaja Mwenyezi Mungu; na useme unapo azimia kufanya jambo na kuliambatanisha na kupenda kwa Mwenyezi Mungu: Huenda Mola wangu Mlezi akaniwafikisha kwenye bora kuliko nililo azimia kufanya, na lenye kuongoka zaidi.

25 Na hakika hao vijana walikaa katika pango lao nao wamelala kwa miaka mia tatu, na ikazidi tisa. (Tazama Maelezo 18:25)

26 Ewe Mtume! Waambie watu: Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kujua zama zao zote. Kwani Yeye *Subhanahu* ndiye aliye khusika kujua siri za mbingu na ardhi. Jinsi gani kulivyo tukuka kuona kwake kwa viumbe vyote! Na jinsi gani kulivyo tukuka kusikia kwake kwa kila cha kusikilizana! Na

27. Na soma uliyo funuliwa katika Kitabu cha Mola wako Mlezi. Hapana wa kubadilisha maneno yake. Wala nawe hutapata makimbilio isipo kuwa kwake.²⁷

28. Na isubirishe nafsi yako pamoja na wanao muomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka radhi yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia. Wala usimt'ii tuliye mghafilisha moyo wake asitukumbuke, na akafuata matamania yake yakawa yamepita mpaka.²⁸

29. Na sema: Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae. Hakika Sisi tumewaandalia wenye kudhulumu Moto ambao utawazunguka kama khema. Na wakiomba msaada watasaidiwa kwa kupewa maji kama mafuta yaliyo tibuka. Yatayo wababua nyuso zao. Kinywaji hicho ni kiovu mno! Na matandiko hayo ya kupumzikia ni maovu mno!²⁹

30. Hakika wale walio amini na wakatenda mema - hakika Sisi hatupotezi ujira wa anaye tenda mema.³⁰

31. Hao watapata Bustani za milele, zinazo pita mito kati yake. Humo watapambwa kwa mavazi ya mikononi ya dhahabu, na watavaa nguo za kijani za hariri na at'ilasi, huku wakiegemea humo juu ya makochi. Ni malipo bora hayo! Na matandiko mazuri mno ya kupumzikia!³¹

32. Na wapigie mfano wa watu wawili: mmoja wao tulimpa vitalu viwili vya mizabibu,

hapana katika wa mbinguni na wa katika ardhi wa kuendesha mambo yao isipo kuwa Yeye. Na wala hapana wa kumshiriki katika hukumu yake kiumbe chochote.

27 Ewe Mtume! Soma uliyo funuliwa kwa wahyi katika Qur'ani. Na katika hayo yamo uliyo funuliwa ya khabari za hao vijana. Wala usisikilize hayo maskhara yao ya kutaka ubadilishe muujiza wa Qur'ani kwa muujiza mwingine. Kwani hakika hapana wa kuyageza anayo simulia Mwenyezi Mungu maneno ya haki katika muujiza yake. Hakika hapana awezae kubadilisha hayo. Wala usende kinyume na amri ya Mola wako Mlezi, kwani hapo tena hutapata wa kumkimbilia kukuhifadhi naye.

28 Ewe Mtume! Shikamana na usuhuba wa masahaba wako Waumini, wanao muabudu Mwenyezi Mungu peke yake asubuhi na jioni daima, huku wanataka radhi zake. Wala jicho lako lisiwawache hao kuwaangalia wapinzani wa kikafiri kwa kutaka kustarehe nao katika mapambo ya maisha ya dunia. Wala usikubali kuwafukuza Waumini mafakiri katika baraza yako kwa kumridhisha huyo tuliye mghafilisha moyo wake na kutukumbuka Sisi, kwa kuwa yeye mwenyewe hakuwa tayari kwa hayo, na akawa ni mtumwa wa pumbao lake, na mambo yake katika vitendo vyake hayakufuata njia iliyo sawa. Na anapo katazwa Nabii, basi ndio wanakatazwa wengineo (yaani sote sisi). Na hakika Nabii s.a.w. hataki maisha ya dunia na pumbao lake. Lakini makatazo hayo anaelekezewa Nabii ili wengine watahadhari na kutaka pumbao la dunia. Kwani ikiwa yaweza kuwa kwake kutaka pumbao la kimwili, basi kila mwanaadamu yaweza kuwa katika nafsi yake. Kwa hivyo ajilinde.

29 Sema ewe Mtume!: Hakika haya niliyo kuja nayo ni kweli tupu iliyo toka kwa Mola wenu Mlezi. Basi anaye taka kuyaamini na ayaamini. Kwani hiyo ni kheri yake mwenyewe. Na anaye taka kuyakataa na akatae. Kwani huyo haidhulumu ila nafsi yake mwenyewe. Hakika Sisi tumekwisha muwekea tayari anaye jidhulumu nafsi yake kwa ukafiri Moto utao mzunguka kama khema. Na hao walio dhulumu wakiomba wasaidiwe kwa maji huko katika Jahannamu, wataletewa maji kama mafuta yaliyo tibuka yamoto mno, hubabua nyuso kwa uvukuto wake! Kinywaji hicho ni kibaya mno, na Jahannamu ni pahali paovu pa mapumziko yao!!

30 Ama wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Dini ya Haki uliyo funuliwa wewe, na wakatenda aliyo waamrisha Mola wao Mlezi, nayo ni vitendo vyema, basi Sisi hatuto wapotezea ujira wao wa vitendo vyema walivyo vitenda.

31 Watu hao watakuwa na Mabustani ambayo watastarehe ndani yake daima dawamu. Kati baina ya miti na majumba yake inapita mito, na watapambiwa yanayo onekana ni ya starehe katika dunia, kama mapambo ya dhahabu, na mavazi yao ni nguo za kijani za hariri za kila namna, wakiegemea juu ya makochi na matakia na mapazia. Watapata malipo bora, na Bustani nzuri ya kudumu na kustarehe. Humo watapata kila wakitakacho.

na tukavizungushia mitende, na kati yake tukatia mimea ya nafaka.³²

33. Na hivyo vitalu viwili vikitoa mazao yake, wala hapana kitu katika hayo kilicho tindikia. Na ndani yake tukapasua mito.³³

34. Naye alikuwa na mazao mengi. Basi akamwambia mwenzake naye akibishana naye: Mimi nimekushinda wewe kwa mali na nguvu za watu!³⁴

35. Na akaingia kitaluni kwake, naye hali anajidhulumu nafsi yake. Akasema: Sidhani kabisa kuwa haya yataharibika.³⁵

36. Wala sidhani kuwa hiyo Saa (ya Kyama) itatokea. Na ikiwa nitarudishwa kwa Mola wangu Mlezi, bila ya shaka nitapata marejeo bora zaidi kuliko haya.³⁶

37. Mwenzake akamwambia kwa kubishana naye: Je! Unamkufuru aliye kuumba kutokana na udongo, tena kutokana na tone la manii, kisha akakufanya mtu kaamili?³⁷

38. Lakini Yeye Mwenyezi Mungu ndiye Mola wangu Mlezi. Wala simshirikishi na yeyote.³⁸

39. Na lau kuwa ulipo ingia kitaluni kwako ungesi sema: Mashaallah! Alitakalo Mwenyezi Mungu huwa! Hapana nguvu ila kwa Mwenyezi Mungu. Ikiwa unaniona mimi nina mali kidogo na watoto kuliko wewe,³⁹

40. Basi huenda Mola wangu Mlezi akanipa kilicho bora kuliko kitalu chako, naye akapitisha kudra yake kutoka mbinguni kukilitea hicho chako, na kikageuka ardhi tupu inayo teleza.⁴⁰

41. Au maji yake yakadidimia wala usiweze kuyagundua.⁴¹

32 Ewe Mtume! Bainisha baina ya hali ya makafiri matajiri na Waumini mafakiri kwa kuwapigia mfano ulio tokea hapo zamani baina ya watu wawili: kafiri na Muumini. Huyu kafiri alikuwa na vitalu viwili vya mizabibu, na tukavizungushia mitende kwa ajili ya pambo na faida pia. Na baina ya hivyo vitalu tukaweka makulima mengine yaliyo stawi na kutoa mazao.

33 Na kila kitalu kikawa kinatoa mazao yake kwa wingi na kubaariki. Wala hapana kilicho tindikia. Na tukapasua mto unamiminika kati yao.

34 Na huyo mwenye vitalu alikuwa na mali mengine yenye kutoa mazao yake pia. Basi ikamuingia ghururi kwa neema ile. Katika ile ghururi yake akamwambia mwenzie yule Muumini nao walikuwa wakijadiliana: Mimi nina mali mengi kuliko wewe, na ninakushinda kwa nguvu za jamaa zangu na wasaidizi.

35 Kisha akaingia katika kitalu chake kimojapo pamoja na yule mwenzie Muumini, naye huku amejaa ghururi, akamwambia: Sidhani kabisa kuwa kitalu hiki kitapotea!

36 Wala sidhani kuwa Kiyama kitakuja. Na pindi ikawa nikirejea kwa Mola wangu Mlezi kwa kufufuliwa kama unavyo dai wewe, basi Wallahi! Hapana shaka nitapata bustani bora kuliko kitalu hiki huko Akhera. Kwani mimi ni mtu wa neema kwa kila hali. Yeye huyu anakisia hayo ya ghaibu kwa haya yaliyoko sasa. Wala hajui kuwa Akhera malipo yake ni kwa Imani na vitendo vya kheri.

37 Mwenzie Muumini akamjibu: Unajiachilia kumkufuru Mola wako Mlezi aliye kuumba tangu asli yako ya Adam kutokana na udongo, kisha kutokana na tone ya maji-maji ya mbegu ya uzazi, kisha akakufanya mtu aliye kamilika? Ikiwa unajiona bora kwa mali yako na jamaa zako, basi mkumbuke Mola wako Mlezi na asli yako ya udongo.

38 Lakini mimi ninasema: Hakika aliye niumba mimi na akaumba ulimwengu wote huu ni Mwenyezi Mungu Mola wangu Mlezi. Na mimi namuabudu Yeye peke yake, wala simshirikishi na yeyote.

39 Na lau kuwa ungesi sema unapo ingia katika hii bustani yako ya duniani na ukaangalia viliomo ndani yake: Haya Mashaallah! Ndio aliyo yataka Mwenyezi Mungu. Wala mimi sina nguvu ya kuyapata haya bila ya msaada wa Mwenyezi Mungu. Hayo inge kuwa ni shukrani za kupelekea kudumu neema yako. Tena akazidi kumwambia: Ikiwa umeniona mimi ni duni kuliko wewe kwa mali na watoto na wasaidizi...

40 ...basi huenda Mola wangu Mlezi akanipa bora kuliko hiyo bustani yako, hapa duniani au kesho Akhera, na akaipelekea bustani yako kudra yake aliyo ikadiria, kama radi mathalan kutoka mbinguni. Na ikawa ardhi kavu inayo teleza haime kitu, wala unyayo hautulii juu yake.

41 Au maji yake yakazama katika ardhi, yasipatikane, wala usiweze kuyachota kwa kumwagia katika shamba.

42. Yakateketezwa matunda yake, akabaki akipindua pindua viganja vyake, kwa vile alivyo yagharimia, na miti imebwagika juu ya chanja zake. Akawa anasema: Laiti nisingeli mshiriki Mola wangu Mlezi na yeyote!⁴²
43. Wala hakuwa nacho kikundi cha kumsaidia badala ya Mwenyezi Mungu, wala mwenyewe hakuweza kujisaidia.⁴³
44. Huko ulinzi ni wa Mwenyezi Mungu wa Haki tu. Yeye ndiye mbora wa malipo, na mbora wa matokeo.⁴⁴
45. Na wapigie mfano wa maisha ya dunia. Hayo ni kama maji tunayo yateremsha kutoka mbinguni, yakachanganyika na mimea ya ardhi, kisha hiyo mimea ikawa vibuwa vinavyo peperushwa na upepo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.⁴⁵
46. Mali na wana ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini.⁴⁶
47. Na siku tutapo iondoa milima na ukaiona ardhi iwazi, na tukawafufua - wala hatutamwacha hata mmoja kati yao -⁴⁷
48. Na wakahudhurishwa mbele ya Mola wako Mlezi kwa safu (wakaambiwa): Mmetujia kama tulivyo kuumbeni mara ya kwanza! Bali mlidai kwamba hatutakuwekeeni miadi.⁴⁸
49. Na kitawekwa kitabu. Basi utawaona wakosefu wanavyo ogopa kwa yale yaliomo humo. Na watasema: Ole wetu! Kitabu hichi kina nini! Hakiachi dogo wala kubwa ila huliandika? Na watayakuta yote waliyo yatenda yamehudhuria hapo. Na Mola wako Mlezi hamdhulumu yeyote.⁴⁹

42 Mwenyezi Mungu kmpatiliza yule kafiri, akayateketeza mavuno yote ya kitalu chake, na hicho kitalu chenyewe akakiangamiza, na akang'oa hata mizizi yake. Yule kafiri akabakia akipindua pindua viganja vyake kwa kusikitikia gharama alizo zitoa katika kukiamirisha kitalu chake, na baadae kuja kikapatilizwa na uharibifu. Akatamani lau kuwa hakumshirikisha Mola wake Mlezi na yeyote.

43 Katika balaa hii hakuwa na jamaa wa kuja mnusuru badala ya Mwenyezi Mungu kama alivyo kuwa akijitapa. Wala hakuwa anaweza kujisaidia nafsi yake.

44 Kwani katika kila hali nusura iko kwa Mwenyezi Mungu wa Haki peke yake. Na Yeye *Subhanahu* ni Mwema kwa mja wake Muumini, humkirimu kwa malipo, na humfanyia mema matokeo yake.

45 Ewe Mtume! Watajie watu mfano wa maisha ya duniani, vipi uzuri wake na kupendeza kwake, na mara hupotelea mbali. Ni kama mfano wa maji yanayo teremka kutoka mbinguni yakamwagiwa mimea ikanawiri, ikastawi. Kisha punde si punde ikakauka, ikawa vibua vikavu vilivyo katika katika vikipeperushwa na upepo. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuleta na kuondoa akitakacho.

46 Mali na wana ni pambo na starehe kwenu katika uhai wa duniani, na pia ndio nguvu zenu. Lakini vyote hivyo havina dawamu. Hivyo vina mwisho wake, havibakii. Na vitendo vyema vyenye kubaki ni bora kwenu mbele ya Mwenyezi Mungu. Yeye hukumimieni kwa ukarimu thawabu zake, na hivyo ndio bora ya matumaini ya binaadamu.

47 Na ewe Mtume! Waonye watu kwa Siku ambayo vyote viliopo vitaondoka. Milima itaondoka, na mtaiona ardhi tupu wazi imetanda, hapana chochote kilicho kuwapo cha kuisitiri. Na tutawafufua watu kwa ajili ya hisabu, na hatutamwacha hata mmoja kati yao.

48 Na Siku hii watu watahudhurishwa kwa makundi wakipangwa kwa masafu kwa ajili ya hisabu. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema: Tumekufueni kutokana na mauti, kama tulivyo kuumbeni pale mara ya mwanzo. Na mmetujia peke yenu, mmoja, mmoja, bila ya mali, na bila ya wana. Na duniani mlikuwa mkikanusha kufufuliwa na kuhisabiwa.

49 Na katika mkono wa kila mmojapo kitawekwa kitabu cha vitendo vyake. Waumini watakiona na watafurahi kwa yaliyomo humo. Na wakanushaji wataona nao wamejaa khofu kwa vitendo viovu viliomo humo. Watasema wakisha ona hayo: Hilaki gani hii! Tunastaajabia kitabu hichi hakikuacha hata dogo katika vitendo vyetu, wala kubwa, ila kimetuandikia! Na wataona malipo ya waliyo yatenda ni ya haki.

- 50.** Na tulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam! Walimsjudia isipo kuwa Iblisi. Yeye alikuwa miongoni mwa majini, na akavunja amri ya Mola wake Mlezi. Je! Mnamshika yeye na dhuriya zake kuwa marafiki badala yangu, hali wao ni adui zenu? Ni ovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu.⁵⁰
- 51.** Sikuwashuhudisha kuumbwa kwa mbingu na ardhi, wala kuumbwa kwa nafsi zao. Wala sikuwafanya wapotezao kuwa ni wasaidizi.⁵¹
- 52.** Na siku atakapo sema (Mwenyezi Mungu): Waiteni hao mlio dai kuwa ni washirika wangu. Basi watawaita, na wao hawato waitikia. Nasi tutaweka baina yao maangamio.⁵²
- 53.** Na wakhaliifu watauona Moto na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuuepuka.⁵³
- 54.** Na bila ya shaka tumewaelezea watu katika hii Qur'ani kila namna ya mfano. Lakini mwanaadamu amezidi kuliko kila kitu kwa ubishi.⁵⁴
- 55.** Na hapana kilicho wazuia watu kuamini ulipo wajia uwongofu na wakaomba maghfira kwa Mola wao Mlezi, isipo kuwa yawafikie ya wale wa zamani, au iwafikie adhabu jahara.⁵⁵
- 56.** Na hatuwatumi Mitume ila wawe wabashiri na waonyaji. Na walio kufuru wanabishana kwa uwongo, ili kwa uwongo huo waivunje kweli. Na wanazifanya Ishara zangu na yale waliyo onywa kuwa ni mzaha.⁵⁶
- 57.** Na ni nani dhaalimu mkubwa zaidi kuliko yule anaye kumbushwa Ishara za Mola wake Mlezi, naye akazipuza na akasahau yaliyo tangulizwa na mikono yake? Hakika Sisi tumeweka vifuniko juu ya nyoyo zao ili wasifahamu, na uziwi kwenye masikio

Wala Mola wako Mlezi hamdhulumu yeyote katika waja wake.

50 Ewe Mtume! Watajie mwanzo wa kuumbwa kwao, ili wajue kuwa wao wametokana na udongo, basi wasikae wakidanganyika na hayo waliyo nayo, wakamnyenyekea Iblisi, adui wa baba yao. Kwani yeye alikuwa katika majini, akajivuna, na akamuasi Mwenyezi Mungu. Basi yawaje baada ya kwisha jua khabari zake mkamfanya yeye na kizazi chake kuwa ndio wasaidizi wenu badala ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio adui zenu! Badala hii ni ovu kwa mwenye kuidhulumu nafsi yake na akamt'ii Shetani.

51 Mimi sikumwonyesha Iblisi wala dhuriya zake nilipo umbwa mbingu wala ardhi, wala sikuwashuhudisha baadhi yao nilipo waumba wenzao ili wanisaidie. Wala sikuwa nina haja ya msaidizi wowote, licha kuwa nikatafute wapotovu ndio wawe wasaidizi wangu. Basi yawaje mnakwenda mt'ii Shetani na mkaniasi Mimi?

52 Watajie siku atayo waambia Mwenyezi Mungu washirikina: Waiteni hao mlio kuwa mkidai duniani kuwa ni washirika wangu katika ibada ili wakuombeeni kwa mujibu wa madai yenu. Nao watawaita, na hao hawato waitikia. Nasi tumejaalia sasa hapana baina yao ila ni maangamio tu kwa makafiri, baada ya kuwa duniani walikuwa na mawasiliano ya ibada na mapenzi.

53 Na wakosefu watauona Moto na watayakinika kuwa hapana shaka watauingia tu. Wala hawatakuwa na pahala pengine badala yake.

54 Na Mwenyezi Mungu amewatajia watu katika Qur'ani hii, wanayo ikanusha na wakataka waletewe muujiza mwenginewe, mifano namna kwa namna, ili wapate kuwaidhika kwayo. Lakini mwanaadamu tabia yake ni kupenda kubishana. Akiwa kafiri basi atabisha hata kwa uwongo.

55 Na hapana lililo wazuia washirikina kuamini zilipo wafikia sababu za kuongoka, nazo ni huyu Mtume na Qur'ani, isipo kuwa ukaidi wao na kumtaka Mtume awalettee aliyo walettea Mwenyezi Mungu wale watu wa zamani, nayo ni kuangamizwa moja kwa moja kama kulio wapata hao wa kale, au awalettee adhabu ya dhaahiri hivi.

56 Lakini Mwenyezi Mungu hawatumi Mitume wake ila kwa ajili ya kutoa bishara njema na kuonya. Wala hawatumi kwa ajili ya hao wenye inda wawatake walettee muujiza makhsusi. Lakini walio kufuru wanaacha hoja, na wanabishana na Mitume kwa upotovu ili waipotoe Haki. Na msimamo wao kwa Qur'ani na maonyo ni msimamo wa mwenye kejele na maskhara ambaye hana makusudio ya kutafuta hakika ya mambo.

yao. Na ukiwaita kwenye uwongofu hawakubali kabisa kuongoka.⁵⁷

58. Na Mola wako Mlezi ni Msamehevu Mwenye rehema. Lau angeli wachukulia kwa mujibu waliyo yachuma, bila ya shaka angeli wafanyia haraka kuwaadhibu. Lakini wanayo miadi ambayo hawatapata makimbilio yoyote ya kuepukana nayo.⁵⁸

59. Na miji hiyo tuliwaangamiza watu wake walipo dhulumu. Na tukawawekea miadi ya maangamizo yao.⁵⁹

60. Na pale Musa alipo mwambia kijana wake: Sitoacha kuendelea mpaka nifike zinapo kutana bahari mbili, au nitaendelea kwa muda mrefu.⁶⁰

61. Basi wawili hao walipo fika zinapo kutana hizo bahari mbili walimsahau samaki wao, naye akashika njia yake kaporonyokea baharini.⁶¹

62. Walipo kwisha pita alimwambia kijana wake: Tupe chakula chetu cha mchana. Kwa hakika tumepata machofu kweli kwa hii safari yetu.⁶²

63. Akasema (kijana): Waona! Pale tulipo pumzika penye jabali basi mimi nilimsahau yule samaki. Na hapana aliye nisahaulisha nisimkumbuke ila Shet'ani tu. Naye akashika njia yake baharini kwa ajabu.⁶³

64. (Musa) akasema: Hayo ndiyo tuliyo kuwa tunayataka. Basi wakarudi nyuma kwa kufuata njia waliyo jia.⁶⁴

65. Basi wakamkuta mja katika waja wangu tuliye mpa rehema kutoka kwetu, na tukamfunza mafunzo yaliyo toka kwetu.⁶⁵

66. Musa akamwambia: Nikufuate ili unifunze katika ule uwongofu ulio funzwa

57 Na hapana yeyote aliye dhaalimu mkubwa zaidi kuliko huyo anaye waidhiwa kwa Ishara za Mola wake Mlezi naye asizingatie, na akasahau nini matokeo ya maasi yake anayo yatenda! Hakika Sisi kwa sababu ya kuelekea kwao kwenye ukafiri tumeweka vifuniko juu ya nyoyo zao, basi nyoyo zao hazitambui wala haziingii mwangaza. Na masikioni mwao tumetia uziwi basi hawasikii la kuwafahamisha! Nawe, ewe Mtume! Ukiwaita kwenye Dini ya Haki hawato ongoka maadamu tabia yao ni hii.

58 Na Mola wako Mlezi Mtukufu Mwingi wa kusamehe makosa ya waja wake, Mwenye rehema kunjufu kwa mwenye kumuelekea, lau angeli penda kuwatwaa kwa maovu wayatendayo basi angeli wapatiliza upesi upesi kama alivyo kwisha watangulizia wenginewe. Lakini hii ni hikima yake aliyo ikadiria. Anawaakhirisha mpaka ufike wakati atapo waonjesha adhabu kali kabisa. Na hapo hawatopata pa kukimbilia na kuwalinga.

59 Na hii basi ndio miji ya kale tuliyo iteketeza pale watu wao walipo dhulumu kwa kuwakanusha Mitume wao. Na Sisi tukawawekea miadi ya kuwaangamiza isiyo na khitilafu. Hali kadhaalika itakuwa ya hao katika kaumu yako wanao kanusha, ikiwa hawaamini.

60 Na hakika hapana mtu anaye jua ya Mwenyezi Mungu ila Yeye Mwenyewe anapo mpa kipawa hicho Nabii au mtu mwema. Ewe Mtume! Simulia kuwa Musa bin Amran alimwambia kijana wake, mtumishi wake, mwanafunzi wake: Sitoacha kwenda mpaka nifike zinapo kutana bahari mbili, au basi nitaendelea kwenda tu muda mrefu.

61 Basi Musa na kijana wake walipo fikilia pahala panapo kusanyika bahari mbili wakamsahau samaki wao walio kuwa wamemchukua kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Akatumbukia baharini, akashika njia yake katika maji!

62 Musa na kijana wake walipo fika mbali na pahala pale, na wakaona njaa na machofu Musa akamwambia kijana wake: Tupe cha kukila. Hakika tumepata taabu na mashaka katika safari yetu hii.

63 Kijana wake akasema: Unakumbuka? Pale tulipo pumzika kwenye lile jabali, basi mimi nilimsahau yule samaki. Na hapana aliye nisahaulisha ila Shetani. Na hapana shaka samaki yule katumbukia baharini. Na mimi hakika najistaajabia kusahau kwangu huku.

64 Musa akamwambia: Haya yaliyo tokea ndiyo tuliyo kuwa tunayataka kwa mujibu wa hikima anayo itaka Mwenyezi Mungu. Basi wakarejea nyuma kwa njia yao ile ile waliyo jia, wakizifuata nyayo zao.

65 Mpaka wakafika kwenye lile jabali. Hapo wakamkuta mja miongoni mwa waja wangu walio wema, tuliye mpa hikima, na tukampa ujuzi mwingi kutokana kwetu.

wewe?⁶⁶

67. Akasema: Hakika wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami.⁶⁷

68. Na utawezaje kuvumilia yale usiyo yajua vilivyo undani wake?⁶⁸

69. Akasema: *Inshaallah*, Mwenyezi Mungu akipenda, utaniona mvumilivu, wala sitoasi amri yako.⁶⁹

70. Akasema: Basi ukunifuata usiniulize kitu mpaka mimi nianze kukutajia.⁷⁰

71. Basi wawili hao wakatoka, hata walipo panda jahazi (yule mtu) akaitoboa. (Musa) akasema: Unaitoboa uwazamisha watu wake? Hakika umefanya jambo baya.⁷¹

72. Akasema: Sikukwambia hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?⁷²

73. (Musa) akasema: Usinichukulie kwa niliyo saha, wala usinipe uzito kwa jambo langu.⁷³

74. Basi wakatoka wawili hao mpaka wakamkuta kijana, akamuwa. (Musa) akasema: Ala! Umemuwa mtu asiye na kosa, na wala hakuwa! Ama hakika umefanya jambo baya kabisa!⁷⁴

75. AKASEMA: Je! Sikukwambia kwamba hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami?⁷⁵

76. Akasema: Nikikuuliza kitu chochote baada ya haya usifuatane nami, kwani umekwisha pata udhuru kwangu.⁷⁶

77. Basi wakatoka mpaka wakawafikia watu wa mji mmoja. Wakawaomba watu wake wawape chakula, nao wakakataa kuwakaribisha. Hapo wakakuta ukuta unataka kuanguka, (yule mja mwema) akausimamisha. (Musa) akasema: Ungeli taka ungelichukua ujira kwa haya.⁷⁷

78. (Yule mtu) akasema: Huku ndio kufarikiana baina yangu na wewe. Sasa nitakueleza

66 Musa akamwambia yule mja mwema: Je nende nawe upate kunifunza nami aliyokufunza Mwenyezi Mungu?

67 Akamwambia hutaweza kustahamili kufuatana nami.

68 Na utawezaje kustahamili jambo lisilo pata kukufika mfano wake.

69 Musa akasema: *Inshaallah*, Mwenyezi Mungu akipenda, utaniona mimi ni mwenye kusubiri, na mt'iifu kwako kwa yote utayo niamrisha.

70 Yule mja mwema akasema: Basi ukunifuata na ukayaona usiyo yafahamu, usiingie kuniuliza mpaka nianze mimi kukusimulia.

71 Wakatoka wakitambaa na mfukwe wa bahari mpaka wakakuta jahazi wakaipanda. Yule mja mwema akaitoboa jahazi ile nayo imo safarini. Musa akapinga kwa kusema: Umeitoboa makusudi upate kuwazamisha watu wake? Ama hakika umefanya jambo ovu!

72 Yule mja mwema akasema: Mimi nilikwisha kwambia kuwa hakika wewe hutoweza kusubiri kuwa nami.

73 Musa akamwambia: Usinichukulie kwa kusahau wasia wako, wala usinikutishe mashaka katika kutafuta ilimu kwako, na ukafanya hiyo kazi nzito.

74 Na baada ya kutoka kwenye jahazi ile wakaingia kuendelea na safari yao. Njiani wakamkuta kijana. Yule mja mwema akamuwa yule kijana! Musa akasema kwa kuchukua: Unakwenda muuwa mtu asiye na kosa lolote, na wala hakumuwa mtu yeyote? Hakika umefanya jambo ovu kweli kweli.

75 Mja mwema akamwambia Musa: Mimi nalikwambia kwamba wewe hutaweza kustahamili ukanyamaza kimya usiniulize.

76 Musa akasema: Nikikuuliza lolote baada ya mara hii basi usifuatane nami, kwani umekwisha filikia kiwango cha kupata udhuru wa kutokuwa nami.

77 Wakanda hata wakafika kwenye mji. Wakawataka watu wake wawape chakula, wakakataa kuwakirimu. Wakakuta ukuta umeinama wakaribia kuanguka. Yule mja mwema akauadiriki. Akaujenga mpaka akausimamisha sawa. Musa akasema: Ungeli taka ungeliveza kudai ujira kwa kazi uliyo ifanya.

maana ya yale uliyo kuwa huwezi kuyastahamia.⁷⁸

79. Ama ile jahazi ilikuwa ya masikini za Mungu wafanyao kazi baharini. Nilitaka kuiharibu, kwani nyuma yao alikuwako mfalme anaghusubu majahazi yote.⁷⁹

80. Na ama yule kijana, wazazi wake walikuwa ni Waumini. Tukakhofu asije watia mashakani kwa uasi na ukafiri.⁸⁰

81. Basi tulitaka Mola wao Mlezi awabadilishie aliye bora zaidi kuliko huyo kwa kutakasika, na aliye karibu zaidi kwa huruma.⁸¹

82. Na ama ukuta, huo ulikuwa ni wa vijana wawili mayatima kule mjini. Na chini yake ilikuwako khazina yao; na baba yao alikuwa ni mtu mwema. Basi Mola wako Mlezi alitaka wafikie utu uzima na wajitolee khazina yao wenyewe, kuwa ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi. Wala mimi sikutenda hayo kwa amri yangu. Hiyo ndiyo tafsiri ya hayo ambayo wewe hukuweza kuyasubiria.⁸²

83. Na wanakuuliza khabari za Dhul- Qarnaini. Waambie: Nitakusimulieni baadhi ya hadithi yake.⁸³

84. Sisi tulimtilia nguvu katika ardhi na tukampa njia za kila kitu.⁸⁴

85. Basi akaifuata njia.⁸⁵

86. Hata alipo fika machwea-jua aliliona linatua katika chemchem yenye matope meusi. Na hapo akawakuta watu. Tukasema: Ewe Dhul-Qarnaini! Ama uwaadhibu au watwae kwa wema.⁸⁶

87. Akasema: Ama aliye dhulumu basi tutamuadhibu, na kisha atarudishwa kwa Mola wake Mlezi amuadhibu adhabu isiyo juulikana.⁸⁷

78 Mja mwema akasema: Huku kutaaradhi kwako mara kwa mara kwa niyatendayo mimi ndio sababu ya kufarikiana mimi nawe. Sasa basi nitakueleza hikima ya yote haya ambayo wewe huyajui undani wake, wala hukuweza kuyasubiria yaliyo fichikana ukangojea kujua hakika yake na siri yake.

79 Ama ile jahazi niliyo itoboa ilikuwa ni ya watu wanyonge wenye haja, ambao kazi yao ni ya baharini wakitafuta riziki yao. Basi mimi nikataka kukitia ila chombo chao kisitakikane. Kwani nyuma yao yuko mfalme mtindo wake ni kupokonya kila jahazi nzima. (Kughusubu, kupokonya, hata kukiitwa “kutaifisha” ni dhambi kubwa kabisa kwa Mwenyezi Mungu, kwani ni dhulma.)

80 Ama yule kijana niliye muuwa, baba yake na mama yake walikuwa ni Waumini. Tulikuwa tunajua kuwa angeli ishi angeli kuwa ndio sababu ya ukafiri wao.

81 Basi tukataka kwa kumuwa huyo mtoto Mwenyezi Mungu awape badala yake aliye bora zaidi kwa dini, na mwema zaidi, na mwenye huruma.

82 Ama ule ukuta nilio usimamisha, bila ya ujira, ulikuwa wa vijana wawili mayatima katika watu wa ule mji. Na chini yake ilikuwako khazina walio achiwa na baba yao. Naye alikuwa ni mtu mwema. Basi Mwenyezi Mungu alitaka kuwahifadhia khazina yao ile mpaka wakue wawe na akili zao, na wajitolee wenyewe khazina yao kuwa ni rehema kwao, na kumtukuza baba yao kwa kupitia dhuriya zake. Nami sikufanya niliyo yafanya kwa jitahada ya nafsi yangu. Bali nimefanya hayo kwa kuongozwa na Mwenyezi Mungu. Hii ni tafsiri ya hayo yaliyo fichikana kwako wewe Musa, nawe usiweze kuyavumilia.

83 Ewe Mtume! Baadhi ya makafiri wanakuuliza khabari za Dhul-Qarnaini. Waambie nitakusimulieni baadhi ya khabari zake.

84 Tumemtilia nguvu amri yake katika ardhi, akiendesha humo mambo kwa mazingatio yake na utawala wake. Na tukampa ujuzi mwingi kwa njia ambazo kwazo akiweza kuongoza mambo.

85 Kwa kutumia njia hizo aliweza kuenzea madaraka yake katika ardhi, na akafuata njia mpaka akafika huko magharibi kunako kucha jua.

86 Akenda mpaka akafika pahala mbali huko upande wa magharibi, akalikuta jua kwa linavyo onekana kwa macho kama kwamba linazama pahala penye chemchem ya maji ya moto na matope meusi. Na karibu ya chemchem hii Dhul- Qarnaini aliwakuta watu makafiri. Mwenyezi Mungu akamtia moyoni mwake afanye mojawo ya mambo mawili: Ama awaite kwenye Imani, na hili kwa hakika ni jambo zuri; au awapige vita ikiwa hawakuitikia wito wa Imani.

87 Dhul-Qarnaini akawatangazia: Katika wao aliye jidhulumu nafsi yake kwa kubakia katika ushirikina,

88. Na ama aliye amini na akatenda mema basi atapata malipo mazuri. Nasi tutamwambia lilio jepesi katika amri yetu.⁸⁸
89. Kisha akaifuata njia.⁸⁹
90. Hata alipo fika matokeo ya jua aliliona linawachomozea watu tusio wawekea pazia la kuwakinga nalo.⁹⁰
91. Ndio hivyo hivyo. Na Sisi tulizijua vilivyo khabari zake zote.⁹¹
92. Kisha akaifuata njia.⁹²
93. Hata alipo fika baina ya milima miwili, alikuta nyuma yake watu ambao takriban hawakuwa wanafahamu lolote.⁹³
94. Wakasema: Ewe Dhul-Qarnaini! Hakika Juju-wa-maajuju wanafanya uharibifu katika nchi. Basi je, tukulipe ujira ili utujengee baina yetu na wao ngome?⁹⁴
95. Akasema: Yale Mola wangu aliyo niwezesha ni bora zaidi. Lakini nyinyi nisaidieni kwa nguvu zenu. Nitakujengeeni kizuizi baina yenu na wao.⁹⁵
96. Nileteeni vipande vya chuma. Hata alipo ijaza nafasi iliyo kati ya milima miwili, akasema: Vukuteni. Hata alipo kifanya (chuma) kama moto akasema: Nileteeni shaba iliyo yayuka niimwagie.⁹⁶
97. Basi hawakuweza kuukwea, wala hawakuweza kuutoboa.⁹⁷
98. Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu Mlezi. Na itapo fika ahadi ya Mola wangu Mlezi atauvunja vunja. Na ahadi ya Mola wangu Mlezi ni kweli tu.⁹⁸
99. Na siku hiyo tutawaacha wakisongana wao kwa wao. Na baragumu litapulizwa, na

basi amestahiki adhabu ya duniani kutokana naye, na kisha atarejea kwa Mola wake Mlezi. Naye atamuadhibu adhabu kali wasio ijua.

88 Na ama mwenye kumuitikia, na akamuamini Mola wake Mlezi, na akatenda mema, basi atapata malipo mazuri Akhera, na hapa duniani tunamchukulia kwa upole na wepesi.

89 Kisha Dhul-Qarnaini akaendelea vile vile huku akiomba tawfiki ya Mwenyezi Mungu, na akafuata njia ya kufikilia matokeo jua upande wa mashariki.

90 Hata akafika linapo chomoza jua, kwa ionekanavyo kwa macho, mwisho wa majenzi. Akawaona watu wanaishi katika ushenzi kabisa. Hawana hata cha kuwasitiri na joto.

91 Na kama Dhul-Qarnaini alivyo waita watu wa magharibi waje kuamini basi kadhaalika aliwaita hawa, na akenda nao mwendo ule ule wake wa mwanzo.

92 Kisha akaendelea vile vile akitumia mbinu alizo msahilishia Mwenyezi Mungu za kumpa tawfiki, akishika njia baina ya mashariki na magharibi.

93 Mpaka akafika - katika safari yake ya tatu - pahala mbali baina ya milima miwili mirefu...Na huko akakuta watu ambao hawafahamu wanalo ambiwa ila kwa uzito na mashaka. (*Tazama Maelezo 18:93*)

94 Walipo ziona nguvu zake na uwezo wake wakamtaka awasimamishie ngome ya kuwalinda na Juju-wa-maajuju. Nao hao ni watu wanao waonea maya, na wanawafisidia na kuwaharibia nchi yao. Na wao walikuwa watayari wamlipe ujira kwa kazi hiyo.

95 Akawajibu kwa kuwaambia: Mali na madaraka aliyo nijaalia Mwenyezi Mungu ni bora zaidi kuliko hayo mnayo taka kunipa. Akaanza kusimamisha hiyo ngome, na akawataka wamsaidie kama wawezavyo kwa watu na zana ili awatimizie wayatakayo.

96 Akawataka wamkusanyie vipande vya chuma. Wakakusanya kama alivyo taka. Akajenga kwa hivyo ngome ndefu iliyo lingana na kingo za milima hiyo miwili. Kisha akawaamrisha wawashe moto, wakauwasha, mpaka chuma kikayayuka. Tena akamimina juu yake shaba iliyo kwisha yayushwa; ikawa ngome madhubuti, haipitiki.

97 Basi wale mahasidi hawakuweza kulikwea lile boma, jinsi lilivyo kwenda juu, wala kulitoboa kwa ugumu wake.

98 Dhul-Qarnaini alipo kwisha jenga ile ngome alisema kumshukuru Mwenyezi Mungu: Ngome hii ni rehema iliyo toka kwa Mola wangu Mlezi kwa ajili ya waja wake. Na itabaki hivi hivi imesimama mpaka ije amri ya Mwenyezi Mungu kuiteketeza. Hapo tena itakuwa sawa sawa na ardhi. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni lazima itimie bila ya muhali.

wote watakusanywa pamoja.⁹⁹

100. Na siku hiyo tutawadhihirishia wazi Jahannamu makafiri waione.¹⁰⁰

101. Wale ambao kwamba macho yao yalikuwa paziani hayanikumbuki, na wakawa hawawezi kusikia.¹⁰¹

102. Je, wanadhani walio kufuru ndio wawafanye waja wangu ndio walinzi wao badala yangu Mimi? Hakika Sisi tumeiandaa Jahannamu iwe ndipo mahala pa kuteremkia makafiri.¹⁰²

103. Sema: Je, tukutajieni wenye khasara mno katika vitendo vyao?¹⁰³

104. Ni wale ambao juhudi yao katika maisha ya dunia imepotea bure, nao wanadhani kwamba wanafanya kazi nzuri.¹⁰⁴

105. Hao ni wale walio zikanusha Ishara za Mola wao Mlezi na kukutana naye. Kwa hivyo vitendo vyao vimepotea bure, na wala Siku ya Kiyama hatutawathamini kitu.¹⁰⁵

106. Hiyo Jahannamu ni malipo yao kwa walivyo kufuru na wakafanyia kejeli Ishara zangu na Mitume wangu.¹⁰⁶

107. Hakika wale walio amini na wakatenda mema mashukio yao yatakuwa kwenye Pepo za Firdausi.¹⁰⁷

108. Watadumu humo; hawatataka kuondoka.¹⁰⁸

109. Sema: Lau kuwa bahari ndio wino kwa maneno ya Mola wangu Mlezi, basi bahari ingeli malizika kabla ya kumalizika maneno ya Mola wangu Mlezi, hata tungeli ileta mfano wa hiyo kuongezea.¹⁰⁹

110. Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu

99 Na tangu kujengwa boma hilo Juju-wa-maajuju wakabaki nyuma yake wakipambana wenyewe kwa wenyewe, na wengine wakasalimika na shari yao. Ikifika Siku ya Kiyama likapulizwa baragumu Mwenyezi Mungu atawakusanya viumbe wote kwa ajili ya hisabu na malipo.

100 Na hapo Mwenyezi Mungu atawaonyesha wazi makafiri Jahannamu iwatie kitisho na awatumbukize humo.

101 Na hayo ni kwa kuwa macho yao walipo kuwa duniani yalikuwa yameghafilika hayaoni Ishara za Mwenyezi Mungu kama kwamba yamezibwa na pazia; na walikuwa kwa upotovu wao hawawezi kusikia Wito wa Haki, kama mtu aliye kuwa kiziwi. (Tazama Maelezo 18:101)

102 Je, macho ya makafiri yamepofuka hata wakadhani kwamba kuwafanya watumwa wangu, Malaika na Isa, kuwa ni miungu, wakiwaabudu badala yangu Mimi, kutawapa manufaa na kuwakinga na adhabu? Hakika Sisi tumewaandalia Jahannamu ndio pahali pao pa kukaa wapate huko malipo wanayo yastahiki.

103 Ewe Mtume! Waambie hawa makafiri: Je, nikutajieni watu watao pata khasara mno kwa vitendo vyao na watao kosa thawabu?

104 Ni hao vilio haribika vitendo vyao katika maisha ya duniani kwa kuharibika itikadi yao, na hali wao wanaitakidi kuwa ndio wanafanya vitendo vyema!

105 Hao ndio walio zikataa dalili za uwezo wa Mwenyezi Mungu, na wakaikanusha Siku ya kufufuliwa na kuhisabiwa. Basi vitendo vyao vimepotea bure, na Siku ya Kiyama watastahiki kudharauliwa na kupuuzwa, kwani hawana a'mali ya kutiwa maanani!

106 Hayo ndiyo tuliyo yabainisha na tukayapambanua, hali ya hawa; na malipo yao kwa hayo ni Jahannamu kwa sababu ya kufuru zao na kuzifanyia maskhara Ishara za Mwenyezi Mungu alizo ziteremsha, na Mitume alio watuma.

107 Hakika walio thibiti katika Imani na wakatenda mema, malipo yao ni Bustani za Firdausi watazo ziingia.

108 Wataneemeka milele, wala hawatataka badala yake chochote.

109 Ewe Mtume! Waambie watu: Hakika ujuzi wa Mwenyezi Mungu umekusanya kila kitu. Na lau kuwa maji ya baharini ni wino wa kuandikia maneno ya Mwenyezi Mungu yanayo onyesha ujuzi wake na hikima yake, basi wino huo ungelizika, na hata ungelizika ongezwa wino mwingine kama huo, kabla ya kumalizika maneno ya Mwenyezi Mungu!

Sura 18 - Al-Kahf

wenu ni Mungu Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi.¹¹⁰

110 Ewe Mtume! Waambie watu: Hakika mimi ni mtu tu kama nyinyi, nimetumwa kwenu, nikufunzeni aliyo nifunza Mwenyezi Mungu. Nimefunuliwa (yaani nimepewa Wahyi) ya kwamba Mungu wenu ni Mmoja, hana mshirika wake. Anaye tumai kukutana na Mwenyezi Mungu na kupata malipwa yake, basi naatende vitendo vyema kwa usafi wa niya, na ajitenge mbali na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote katika ibada.

Sura 19 - Maryam

Utangulizi

Hii ni Sura iliyo teremka Makka, na hamna Aya za Madina ila Aya 57 na 71. Hisabu ya Aya zake ni 98. Imeanzia kwa harufi moja moja kama Sura nyingi nyenginezo. Ndani ya Sura hii kipo kisa cha kuzaliwa Yahya bin Zakariya (*Alayhima Ssalam*). Zakariya alitamani mwana na hali kesho fikilia ukongwe na mkewe ni tasa. Na kimetajwa pia kisa cha Bibi Bikra Maryam (A.S.) na kumzaa kwake Masihi (A.S.). Kisha kikatajwa kisa cha Ibrahim (A.S.) na Wito wake kulingania Upweke wa Mwenyezi Mungu, na alivyo mtaka babaake aache kuabudu masanamu, na majibizano yao yaliyo jiri kwa ajili ya masanamu, na madaraka ya Shet'ani.

Pia wameashiriwa Manabii wengine katika dhuriya za Ibrahim, nao Ismail na Is-haq na dhuriya wa Is-haq. Tena kikagusiwa kisa cha Idris (A.S.). Na tena Mwenyezi Mungu *Subhanahu* akataja khabari za walio fuatia wakaja baada ya Manabii, watu wat'iifu na wengine waasi. Na akataja kuwa Pepo ndiyo malipo ya Waumini, na Moto ni malipo ya makafiri, na akazitaja hali za makafiri katika Jahannamu. Na tena *Subhanahu* akagusia ya wapotovu wanao sema kwamba Mwenyezi Mungu ana mwana.

Na *Subhanahu* amebainisha cheo cha Qur'ani, na amewaonya makafiri, na amepiga mifano ya watavyo teketea wanao waasi Manabii. Na akaashiria kwamba hao wamepotea kabisa, hawakuacha hata ukumbusho.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Kaf Ha Ya A'yn S'ad¹
2. Huu ni Ukumbusho wa rehema ya Mola wako Mlezi kwa mja wake, Zakariya.²
3. Alipo mwita Mola wake Mlezi kwa siri.³
4. Akasema: Mola wangu Mlezi! Mafupa yangu yamedhoofika, na kichwa kinameremeta kwa mvi; wala, Mola wangu Mlezi, sikuwa mwenye bahati mbaya kwa kukuomba Wewe.⁴
5. Na hakika mimi nawakhofia jamaa zangu baada yangu. Na mke wangu ni tasa. Basi nipe mrithi kutoka kwako.⁵
6. Atakaye nirithi mimi na awarithi ukoo wa Yaaqub. Ewe Mola wangu Mlezi!

1 Hizi harufi moja moja za kutamkwa zinaonyesha kuwa Qur'ani ni muujiza ulio undwa kwa harufi, na pia ni kuwazindua watu waisikilize.

2 Ewe Mtume! Hizi ni hadithi za Mola wako Mlezi kwa rehema yake kueleza kisa cha mja wake na Nabii wake, Zakariya.

3 Pale alipo muelekea Mwenyezi Mungu na akamwomba kwa siri wasijue watu.

4 Akasema: Mola wangu Mlezi! Mimi nimekwisha dhoofika, na kichwa changu kimejaa mvi. Na mimi sikuwa na bahati mbaya pale ninapo kuomba, bali bahati yangu siku zote ni nzuri, unaniitikia ninapo kuomba.

5 Na mimi ninaogopa kuwa jamaa zangu hawatashika vyema amri za Dini baada ya kufa kwangu. Na mke wangu bado ni tasa, hazai. Basi niruzuku mwana, kwa fadhila yako, atakaye shika pahala pangu kwa watu wangu baada yangu.

Naumjaalie awe mwenye kuridhisha.⁶

7. (Akaambiwa): Ewe Zakariya! Hakika Sisi tunakubashiria mwana; jina lake ni Yahya. Hatujapata kumpa jina hilo yeyote kabla yake.⁷

8. Akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Vipi nitakuwa na mwana na hali mke wangu ni tasa, na mimi nimesha fikia ukongwe katika uzee?⁸

9. Akasema: Ndio hivyo hivyo amesema Mola wako Mlezi: Haya ni mepesi kwangu. Na hakika Mimi nilikwisha kuumba wewe zamani na hali hukuwa kitu.⁹

10. Akasema: Mola wangu Mlezi nijaalie Ishara. Akasema Ishara yako ni kuwa hutasema na watu kwa masiku matatu, na hali ni mzima.¹⁰

11. Basi akawatokea watu wake kutoka mihirabuni. Akawaashiria: Msabihini Mwenyezi Mungu asubuhi na jioni.¹¹

12. Ewe Yahya! Kishike Kitabu kwa nguvu! Nasi tulimpa hikima angali mtoto.¹²

13. Na tukampa huruma itokayo kwetu, na utakaso, na akawa mchamungu.¹³

14. Na akawa mwema kwa wazazi wake, wala hakuwa jabari mua'si.¹⁴

15. Na amani iwe juu yake siku ya kuzaliwa, na siku ya kufa, na siku ya kufufuliwa.¹⁵

16. Na mtaje Maryamu katika Kitabu, pale alipo jitenga na jamaa zake mahali upande wa mashariki.¹⁶

17. Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Roho wetu, akajifananisha kwake sawa na mtu.¹⁷

18. (Maryamu) akasema: Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema aniepushe nawe, ukiwa ni mchamngu.¹⁸

6 Anirithi ilimu na Dini. Na awarithi Ukoo wa Yaaqub ufalme. Ewe Mola wangu Mlezi! Na mjaalie awe maridhia kwako na kwa watu.

7 Akaitwa: Ewe Zakariya! Sisi tunakubashiria khabari nzuri kuwa utapata mwana, na jina tumemwita: Yahya. Hatujapata kumwita mtu yeyote kwa jina hilo kabla yake.

8 Zakariya akasema kwa mastaajabu: Ewe Mola wangu Mlezi! Vipi nipate mwana, na hali mke wangu ni tasa, na mimi nimo katika miaka ya ukongwe.

9 Mwenyezi Mungu akamfunulia mja wake, Zakariya: Mambo ni kama ulivyo bashiriwa, na kwamba kupewa wewe mtoto juu ya ukongwe wako na utasa wa mkeo ni jambo jepesi kwangu Mimi. Wala usiyaone hayo kuwa ni ya mbali hayawezi kuwa. Kwani Mimi nilikuumba wewe kabla yake, na hali hukuwa kitu chochote.

10 Zakariya akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nijaalie alama ya kuonyesha kuwa nitapata hayo uliyo nibashiria. Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: Alama yako ni kuwa hutaweza kusema muda wa masiku matatu, nawe ni mzima wa hisiya na ulimi.

11 Zakariya akawatokea watu wake kutoka kwenye msala, na akawaashiria wamtakase Mwenyezi Mungu asubuhi na jioni.

12 Yahya akazaliwa, akakua, na kisha akapata wito, na akaamrisha ayatende yaliomo katika Taurati kwa juhudi na kuazimia. Na Mwenyezi Mungu alimpa utotoni mwake ilimu ya Dini na kufahamu hukumu za sharia.

13 Mwenyezi Mungu akampa tabia ya huruma, na utukufu wa nafsi, na akamjenga katika uchamungu.

14 Na Mwenyezi Mungu alimjaalia mwema mno kwa wazazi wake wote wawili, na akiwafanyia hisani. Wala hakumfanya awe jhuri kwa watu, wala awe mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu.

15 Na salama na amani iwe kwake, asipatikane na madhara wala maudhi siku ya kuzaliwa kwake, na siku ya kufa kwake, na siku atapo fufuliwa kuwa hai tena.

16 Ewe Mtume! Taja katika Qur'ani hadithi ya Maryamu, pale alipo jitenga na jamaa zake na watu wote, akenda upande wa mashariki ya pale alipo kuwepo.

17 Akafunga pazia baina yake na hao watu. Mwenyezi Mungu akamtuma Jibril amwendee kwa sura ya mwanaadamu kaamili, ili asishituke kumwona kwa sura yake ya Malaika ambayo hakuizoea.

18 Maryamu akasema: Mimi najilinda kwa Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, anikinge nawe, ikiwa

19. (Malaika) akasema: Hakika mimi ni mwenye kutumwa na Mola wako Mlezi ili nikubashirie tunu ya mwana aliye takasika.¹⁹
20. Akasema: Nitampataje mwana hali mwanaadamu yeyote hajanigusa, wala mimi si kahaba?²⁰
21. (Malaika) akasema: Ndio hivyo hivyo! Mola wako Mlezi amesema: Haya ni mepesi kwangu! Na ili tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu, na Rehema itokayo kwetu, na hilo ni jambo lilio kwisha hukumiwa.²¹
22. Basi akachukua mimba yake, na akaondoka nayo mpaka mahali pa mbali.²²
23. Kisha uchungu ukampeleka kwenye shina la mtende; akasema: Laiti ningeli kufa kabla ya haya, na nikawa niliye sahaulika kabisa!²³
24. Pakatangazwa kutoka chini yake: Usihuzunike! Hakika Mola wako Mlezi amejaalia chini yako kijito kidogo cha maji!²⁴
25. Na litikise kwako hilo shina la mtende, utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu.²⁵
26. Basi kula, na kunywa, na litue jicho lako. Na pindi ukimwona mtu yeyote basi sema: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu ya kufunga; kwa hivyo leo sitasema na mtu.²⁶
27. Akenda naye (mwanawe) kwa jamaa zake amembeba. Wakasema: Ewe Maryamu! Hakika umeleta kitu cha ajabu!²⁷
28. Ewe dada yake Harun! Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba.²⁸
29. Akawaashiria (mtoto). Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika mlezi?²⁹
30. (Mtoto) akasema: Hakika mimi ni mtumwa wa Mwenyezi Mungu. Amenipa Kitabu, na amenifanya Nabii.³⁰

unatarajiwa umche Mwenyezi Mungu, na umwogope.

19 Malaika akasema: Mimi si lolote ila nimetumwa na Mola wako Mlezi niwe ni sababu ya kuwa wewe upate mwana aliye safi wa kheri.

20 Maryamu akasema: Vipi nipate mwana na hajanikaribia mwanamume yeyote, na mimi si kahaba?

21 Malaika akasema: Mambo ni kama unavyo sema: Hakukugusa mwanamume. Mola wako Mlezi amesema: Kukupa mwana bila ya baba ni jambo jepesi kwangu, na hilo liwe ni Ishara kwa watu ya kuonyesha ubora wa uwezo wetu, kama ilivyo kuwa ni rehema kwa mwenye kufuata uwongofu wake. Na huku kuumbwa kwa Isa ni amri iliyo kwisha kadiriwa, ni lazima iwe.

22 Matakwa ya Mwenyezi Mungu yakatimia. Maryamu akachukua mimba ya Isa kwa namna alivyo itaka Mwenyezi Mungu. Akatoka na mimba yake akenda pahala mbali na watu.

23 Machungu ya uzazi yakamchukua mpaka kwenye shina la mtende alitegemee, na apate kujisitiri. Akawaza vipi watavyo udhika watu wake naye kwa haya; akatamani afilie mbali, asahaulike kabisa, wala asitajike.

24 Malaika akamtangazia kutoka pahala kwa chini yake: Usihuzunike kwa upweke wako, na kukosa chakula na cha kukinywa, na maneno ya watu. Mwenyezi Mungu kesho jaalia karibu nawe kijito kidogo.

25 Na hebu tikisa huo mtende, zitakuangukia tende mbivu nzuri. (*Tazama Maelezo 19:25*)

26 Basi kula hizo tende na kunywa maji hayo, na tua roho yako. Na ukikutana na mtu yeyote ambaye hakupendezewa na hali yako hii, basi muashirie kuwa wewe umo katika saumu, na husemi na mtu.

27 Maryamu akenda kwa watu wake naye kambeba Isa. Wakamwambia kwa mastaajabu na kuudhika: Umefanya kitendo kiovu!

28 Ewe wa kizazi cha Harun, aliye kuwa Nabii Mchamngu Mahashumu! Vipi umefanya uliyo yafanya na baba yako hakuwa na tabia mbovu, wala mama yako hakuwa kahaba! (*Tazama Maelezo 19:28*)

29 Akawaashiria yule mtoto waseme naye. Wakasema: Vipi tuzungumze na mtoto mchanga ambaye bado yumo katika ubeleko?

30 Isa alipo sikia maneno yao Mwenyezi Mungu alimtamkisha akasema: Hakika mimi ni mtumwa wa

- 31.** Na amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo. Na ameniusia Sala na Zaka maadamu ni hai,³¹
- 32.** Na nimtendee wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, mwovu.³²
- 33.** Na amani iko juu yangu siku niliyo zaliwa, na siku nitakayo kufa, na siku nitakayo fufuliwa kuwa hai.³³
- 34.** Huyu ndiye Isa mwana wa Maryamu. Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanya shaka.³⁴
- 35.** Haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwa na mwana, *Subhanahu*, Yeye ametakasika! Anapo lihukumia jambo basi huliambia tu: Kuwa! Likawa.³⁵
- 36.** Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi, na Mola wenu Mlezi. Basi muabuduni Yeye. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka.³⁶
- 37.** Lakini makundi yakakhitalifiana wao kwa wao. Basi ole wao hao walio kufuru kwa kuhudhuria Siku iliyo kuu!³⁷
- 38.** Watasikia na wataona vizuri vilioje Siku watakayo tufikia! Lakini madhaalimu sasa wamo katika upotofu ulio dhaahiri.³⁸
- 39.** Na waonye siku ya majuto itapo katwa amri. Nao wamo katika ghafla, wala hawaamini.³⁹
- 40.** Hakika Sisi tutairithi ardhi na walio juu yake. Na kwetu watarejeshwa.⁴⁰
- 41.** Na mtaje katika Kitabu Ibrahim. Hakika yeye alikuwa mkweli, Nabii.⁴¹
- 42.** Alipo mwambia baba yake: Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyo sikia, na

Mwenyezi Mungu. Atanipa Injili, na ataniteuwa niwe Nabii.

31 Atanijaalia na baraka, nikifunza kheri, na nikiwafaa watu, na ananiamrisha nishike Sala, na nitoe Zaka muda wa uhai wangu.

32 Kama alivyo niamrisha niwe mwema kwa mama yangu, wala hakunifanya niwe jabari kwa watu, wala mwenye kumuasi Yeye.

33 Na amani iwe juu yangu kutokana na Mwenyezi Mungu siku ya kuzaliwa kwangu, na siku ya kufa kwangu, na siku ya kufufuliwa kwangu nikawa hai tena.

34 Huyu mwenye kusifiwa kwa sifa hizo ndiye Isa bin Maryamu. Na hii ndiyo kauli ya kweli iliyo mkhusu yeye wanayo ipinga wapotovu na wakamtilia shaka unabii wake hao wenye kutia shaka.

35 Wala haifai wala haingii akilini kuwa Mwenyezi Mungu awe na mwana. Yeye ametakasika na hayo! Shani yake *Subhanahu* ni akipitisha hukumu ya jambo lolote basi alitakalo huwa bila ya muhali, kwa tamko tu la kusema: Kuwa! Na hilo jambo huwa.

36 Na hakika Mwenyezi Mungu ndiye Bwana wangu, na ndiye Bwana wenu. Basi muabuduni Yeye. Wala msimshirikishe na yeyote. Hii ninayo kuitieni ndiyo Njia itakayo kufikishieni kwenye mafanikio.

37 Na juu ya iliyo kwisha tangulia katika kauli ya haki iliyo mkhusu Isa, watu wa Biblia wamekhitalifiana wao kwa wao, na wakazua madhehebu mbali mbali. Na makafiri watapata adhabu kali watapo hudhurishwa Siku ya Hisabu, na wakashuhudia msimamo wa Kiyama, na wakakuta malipo maovu kabisa.

38 Watakuwa na masikio makali, na macho yenye nguvu siku watakayo kutana na Mwenyezi Mungu! Lakini wao hii leo duniani kwa kujidhulumu nafsi zao, na kuacha kwao kunafiika kwa kusikia na kuona, wamo katika upotovu wa kuiacha haki, na hayo ni dhaahiri isiyo na uficho.

39 Ewe Mtume! Wahadharishe hawa wenye kudhulumu na siku watakayo juta kwa kupindukia kwao mipaka katika haki ya Mwenyezi Mungu na haki ya nafsi zao wenyewe! Na hapo hisabu yao itakuwa imekwisha, na malipo wamekwisha yapata! Na hali huko duniani walikuwa wameghafilika na Siku hiyo, hawakusadiki kuwa kutakuwako kufufuliwa na kulipwa.

40 Hebu jamani! Nawajue watu kuwa hakika Mwenyezi Mungu ndiye mrithi wa kuirithi ulimwengu wote na kila kiliomo ndani yake. Na hisabu yao wote ni juu ya Mwenyezi Mungu.

41 Ewe Mtume! Watajie watu katika Qur'ani hadithi ya Ibrahim. Hakika yeye alikuwa mtu mkweli kabisa, katika kauli yake na vitendo vyake, na mwenye kueleza vilivyo khabari za Mwenyezi Mungu.

visivyo ona, na visivyo kufaa chochote?⁴²

43. Ewe baba yangu! Kwa yakini imenifikia ilimu isiyo kufikia wewe. Basi nifuate mimi, nami nitakuongoza Njia Iliyo Sawa.⁴³

44. Ewe baba yangu! Usimuabudu Shet'ani. Hakika Shet'ani ni mwenye kumuasi Mwingi wa Rehema.⁴⁴

45. Ewe baba yangu! Hakika mimi naogopa isikupate adhabu inayo toka kwa Mwingi wa Rehema ukaja kuwa mwenziwe Shet'ani.⁴⁵

46. (Baba) akasema: Unaichukia miungu yangu, ewe Ibrahim? Kama huachi, basi lazima nitakupiga mawe. Na niondokelee mbali kwa muda!⁴⁶

47. (Ibrahim) akasema: Salamun a'laika! Amani iwe juu yako! Mimi nitakuombea msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ananihurumia sana.⁴⁷

48. Nami najitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Na ninamwomba Mola wangu Mlezi; asaa nisiwe mwenye kukosa bahati kwa kumwomba Mola wangu Mlezi.⁴⁸

49. Basi alipo jitenga nao na yale waliyo kuwa wakiyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu, tulimpa Is-haq na Yaaqub, na kila mmoja tukamfanya Nabii.⁴⁹

50. Na tukawapa rehema zetu na tukawajaalia kupewa sifa za kweli tukufu.⁵⁰

51. Na mtaje Musa katika Kitabu. Hakika yeye alikuwa ni mwenye kuchaguliwa, na alikuwa Mtume, Nabii.⁵¹

42 Na taja pale Ibrahim alipo msemeza baba yake kwa upole akimwambia: Ewe baba yangu! Vipi unayaabudu masanamu yasiyo sikia wala hayaoni, wala hayawezi kukuletea kheri wala kukuinga na shari?

43 Ewe baba yangu! Mimi yamenijia kwa njia ya ufunuo (wahyi) wa Mwenyezi Mungu ambayo wewe hukuyapata, ya kumjua Mwenyezi Mungu, na kujua yanayo mlazimu mwanaadamu kwa Mola wake Mlezi. Basi nifuate mimi kwa hayo ninayo kuitia ya Imani, nitakuonyesha Njia Iliyo Nyooka itakayo kufikisha kwenye haki na mafanikio.

44 Ewe baba yangu! Usimt'ii Shetani anaye kuzaini uabudu masanamu. Ni mtindo wa Shetani kumuasi Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema na kuikhalifu amri yake.

45 Ewe baba yangu! Mimi nakuogopea ukiendelea na ukafiri utapatilizwa kwa adhabu kali kutokana na Mwingi wa Rehema, ukawa mwenzio ni Shetani Motoni, wewe unamkaribia, na yeye anakaribia.

46 Baba akasema kumwambia Ibrahim naye kakasirika naye, akimtolea ndaro: Yawaje unawawacha miungu yangu, ewe Ibrahim, na unanitaka nimuabudu Mungu wako? Kama hukusita kuwatukana masanamu basi hapana shaka nitakupiga kwa mawe. Tahadhari nami! Niondokelee kwa muda mrefu, mpaka nipoe hamaki zangu.

47 Ibrahim bado akamtwa pole baba yake akamwaga kwa kusema: Salamun A'laika! Amani iwe juu yako! Nitamwomba Mola wangu Mlezi akuongoe na akusamehe. Na Mola wangu Mlezi amenizoeza kuwa na huruma nami, na kuwa karibu nami.

48 Na hivyo mimi basi nakuondokeeni, na najitenga na hiyo miungu mnayo iabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Nami namuabudu Mola wangu Mlezi tu peke yake, kwa kutaraji kuwa apokee ut'iifu wangu, wala yasipotee matarajio yangu.

49 Ibrahim alipo jitenga na baba yake na kaumu yake na miungu yao, Mwenyezi Mungu alimkirimu kwa kumpa dhuriya wema, juu ya kuwa alikuwa kesho kata tamaa ya kupata watoto. Kwani yeye na mkewe walikwisha kuwa ni wakongwe, si wa kuzaa tena. Mwenyezi Mungu akawatunukia Is-haq, na kutokana na Is-haq akazaliwa Yaaqub, na akawateuwa wote wawili wawe Manabii.

50 Na tukawapa, juu ya cheo cha Unabii, kheri nyingi za Dini na dunia kwa rehema zetu. Na tukawarithisha duniani makumbusho mema ya daima kwa ulimi wa kweli mtukufu wa kutaja sifa zao.

51 Ewe Mtume! Wasomee watu katika Qur'ani hadithi ya Musa. Yeye alikuwa ni mwenye niya safi kwa nafsi yake, na moyo wake, na mwili wake, kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu alimteuwa kwa kumpa Unabii na Utume.

52. Na tulimwita upande wa kulia wa mlima na tukamsogeza kunong'ona naye.⁵²
53. Nasi kwa rehema zetu tukampa nduguye, Harun, awe Nabii.⁵³
54. Na mtaje katika Kitabu Ismail. Bila ya shaka yeye alikuwa ni mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii.⁵⁴
55. Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Sala na Zaka, na alikuwa mbele ya Mola wake Mlezi mwenye kuridhiwa.⁵⁵
56. Na mtaje katika Kitabu Idris. Hakika yeye alikuwa ni mkweli Nabii.⁵⁶
57. Na tulimuinua daraja ya juu.⁵⁷
58. Hao ndio alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii katika uzao wa Adam, na katika uzao wa wale tulio wapandisha pamoja na Nuhu, na katika uzao wa Ibrahim na Israil, na katika wale tulio waongoa na tukawateuwa. Wanapo somewa Aya za Mwingi wa Rehema huanguka kusujudu na kulia.⁵⁸
59. Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Sala, na wakafuata matamano. Basi watakuja kuta malipo ya ubaya.⁵⁹
60. Isipo kuwa walio tubu, wakaamini, na wakatenda mema. Hao, basi, wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa chochote.⁶⁰
61. Bustani za milele alizo waahidi Rahmani waja wake katika siri. Hakika ahadi yake hapana shaka itafika.⁶¹
62. Humo hawatasikia upuuzi, ila Salama tu. Na watapata humo riziki zao asubuhi na jioni.⁶²

52 Nasi tulimtukua, na tukamwita kwenye Mlima wa T'ur. Musa akasikia huo wito wa Mwenyezi Mungu kwa upande wa kulia. Nasi tukamkaribisha kwa kumtukua, na tukamteuwa ili tunong'one naye.

53 Tukampa rehema yetu na neema yetu, na tukamchagua pamoja naye nduguye Harun awe Nabii vile vile, ili amsaidie kufikisha ujumbe.

54 Ewe Mtume! Wasomee watu yaliyomo katika Qur'ani katika kisa cha Ismail. Hakika yeye alikuwa ni mkweli wa kutimiza ahadi yake. Na alimuahidi baba yake kuwa atasubiri pindi akimchinja kama alivyo amrisha na Mwenyezi Mungu. Na akatimiza ahadi yake, na Mwenyezi Mungu akamtotea fidia kondoo badala yake na akamtukua kwa kumpa Utume na Unabii.

55 Na alikuwa akiwaamrisha watu wake kushika Sala na kutoa Zaka, na akawa katika makamo matukufu katika kumridhi Mola wake Mlezi.

56 Ewe Mtume! Wasomee watu yaliyomo katika Qur'ani hadithi ya Idris. Dasturi yake ilikuwa ni ukweli wa kauli, na vitendo, na a'mali. Na Mwenyezi Mungu alimpa utukufu wa Unabii.

57 Na kwa hayo Mwenyezi Mungu alimnyanyua cheo cha juu.

58 Hao walio kwisha tajwa, ni miongoni alio waneemesha Mwenyezi Mungu katika Manabii, katika dhuriya wa Adam na dhuriya wa tulio waokoa pamoja na Nuhu na dhuriya wa Ibrahim kama Ismail; na katika dhuriya wa Yaaqub, kama Manabii wa Wana wa Israil; na miongoni tulio waongoa kwenye Haki na tukawachagua walinyanyue Neno la Mwenyezi Mungu. Hawa pindi wakisikia Aya za Mwenyezi Mungu wanasomewa huingia khofu, na huanguka mpaka chini wakimsujudia Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu.

59 Tena baada ya wateuliwa hawa wakatokea wa vizazi vingine wasio kuwa waongofu kama hao. Wakaacha Sala, wakapuuza kunafika na uwongofu wake, na wakashughulikia maasi. Hawa, basi, watakuja kuta malipo ya maasi yao na upotovu wao duniani na akhera.

60 Lakini watao zidiriki nafsi zao kwa kutubia, na kwa Imani ya kweli, na vitendo vyema, basi Mwenyezi Mungu ataipokea toba yao na atawaingiza Peponi, na atawalipa sawa ujira wao.

61 Bustani hizo za Peponi ni makaazi ya milele kwa mujibu wa ahadi ya *Arrahmani*, Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, kuwaahidi waja wake walio tubia, na wakamuamini kwa ghaibu, bila ya kumwona. Basi wao wataingia humo bila ya shaka yoyote, kwani ahadi ya Mwenyezi Mungu haina kinyume.

62 Na hao katika Bustani hizo za Peponi hawatakuwa na mazungumzo ya upuuzi, wala hawatasikia ila kheri na amani. Na riziki yao ni tele na imedhaminiwa haina ukomo.

63. Hiyo ndiyo Pepo tutayo warithisha katika waja wetu walio kuwa wachamngu.⁶³
64. (Nao watasema:) Wala hatuteremki ila kwa amri ya Mola wako Mlezi. Ni yake Yeye yaliyoko mbele yetu na yaliyoko nyuma yetu, na yaliyomo katikati ya hayo. Na Mola wako Mlezi si mwenye kusahau.⁶⁴
65. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yake. Basi muabudu Yeye tu, na udumu katika ibada yake. Je, mnamjua mwenye jina kama lake?⁶⁵
66. Na mwanaadamu husema: Hivyo, nitakapo kufa, ni kweli nitafufuliwa niwe hai tena?⁶⁶
67. Je! Hakumbuki mwanaadamu ya kwamba tulimuumba kabla, na hali hakuwa chochote?⁶⁷
68. Basi naapa kwa Mola wako Mlezi! Kwa yakini tutawakusanya wao pamoja na mashet'ani; kisha tutawahudhurisha kuizunguka Jahannamu, nao wamepiga magoti!⁶⁸
69. Kisha kwa yakini tutawatoa katika kila kundi wale miongoni mwao walio zidi kumuasi *Arrahmani*, Mwingi wa Rahema.⁶⁹
70. Tena hakika Sisi tunawajua vyema zaidi wanao stahiki kuunguzwa humo.⁷⁰
71. Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia. Hiyo ni hukumu ya Mola wako Mlezi ambayo lazima itimizwe.⁷¹
72. Kisha tutawaokoa wale walio mchamngu; na tutawaacha madhaalimu humo wamepiga magoti.⁷²
73. Na wanapo somewa Aya zetu zilizo wazi, walio kufuru huwaambia walio amini:

63 Na hakika Mwenyezi Mungu huwapa Pepo hiyo iwe yao wale ambao duniani walikuwa ni wachamngu, wakaacha maasi na wakatenda mema yanayo stahiki.

64 Na wakati wanapo ingia wakatulia humo husema kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu: Hatukuingia Peponi, wala hatuondoki kutoka hapa kwenda penginepo, ila kwa amri ya Mwenyezi Mungu na fadhila yake. Kwani Yeye, *Subhanahu*, ndiye Mwenye kumiliki, Mwenye kudabiri, na Mwenye kujua ya mbele yetu na ya nyuma yetu. Wala Yeye Mwenyezi Mungu hasahau kutimiza ahadi yake aliyo waahidi waja wake wachamngu.

65 Kwani Yeye, *Subhanahu*, ndiye Muumba, na Mwenye kumiliki mbingu na ardhi na viliomo baina yake; na ndiye Mwenye kuyaendesha mambo yao yote; na ndiye peke yake Mwenye kustahiki kuabudiwa. Basi muabudu Yeye tu; na ushikilie kumuabudu, nawe hali umesubiri na umetua. Kwani Yeye, *Subhanahu*, ndiye Mwenye kustahiki peke yake kuabudiwa, wala hana mwenzie anaye stahiki kuabudiwa, au kuitwa kwa jina lake.

66 Na mwanaadamu kwa mastaajabu kuwa atafufuliwa husema: Vipi nitafufuliwa niwe hai tena, baada ya kwisha kufa na kuteketea?

67 Vipi huyu binaadamu anamstaajabia Mwenyezi Mungu kuweza kumfufua Akhera, na hakumbuki kwamba Yeye Mtukufu alimuumba duniani naye hakuwa chochote, na hali kurejesha kuumba ni jambo jepesi kuliko kuanza kuumba hapo mwanzo, ukipima kwa akili.

68 Ikiwa hili jambo la kufufuliwa linaonekana ni geni, wanalikataa makafiri, basi naapa kwa Aliye kuumba na akakulea, na akakukiza, Siku ya Kiyama tutawakusanya makafiri pamoja na mashetani wao, walio wazaini hata wakauona ukafiri mzuri, tutawakusanya wote kuizunguka Jahannamu, nao wamepiga magoti kwa udhalili na wingi wa kitisho na kufazaika.

69 Kisha kwa yakini kutoka kila kikundi tutawatoa wale walio shadidi ya ukafiri kumkufuru Mwenyezi Mungu na kumuasi, tutawapeleka wao mbele kwenye adhabu iliyo kali kabisa.

70 Na Sisi tunawajua vyema zaidi kati yao wanao stahiki kuingia Motoni na kuungua humo.

71 Na enyi viumbe! Hapana yeyote kati yenu ila atahudhuria hapo. Muumini atauona Moto na atapita, na kafiri atatumbukia. Amri hii lazima itimizwe, hukumu ya Mwenyezi Mungu imekwisha pita.

72 Tena kwa rehema yetu, tutawakusanya wachamngu na tutawaokoa na Jahannamu. Na tutawaacha humo wale walio dhulumu nafsi zao, wakipiga magoti, kwa kuwaadhibu.

Lipi katika makundi mawili lenye cheo kizuri na lilio bora barazani?⁷³

74. Na kaumu ngapi tuliziangamiza zilizo kuwa na mapambo mazuri zaidi na wazuri zaidi kwa kuwatazama!⁷⁴

75. Sema: Walio katika upotofu basi *Arrahmani* Mwingi wa Rahema atawapururia muda mpaka wayaone waliyo onywa - ama ni adhabu au ni Saa. Hapo ndipo watapo jua ni nani mwenye makao mabaya na mwenye askari dhaifu.⁷⁵

76. Na Mwenyezi Mungu huwazidishia uwongofu wenye kushika uwongofu. Na mema yenye kudumu ni bora katika malipo mbele ya Mola wako Mlezi na yana mwisho mwema.⁷⁶

77. Je, umemwona aliye zikanya Ishara zetu na akasema: Kwa hakika mimi nitapewa mali na wana!⁷⁷

78. Kwani yeye amepata khabari za ghaibu, au amechukua ahadi kwa *Arrahmani* Mwingi wa Rehema?⁷⁸

79. Hasha! Tutaandika anayo yasema, tutamkunjulia muda wa adhabu.⁷⁹

80. Na tutamrithi hayo anayo yasema, na atatufikia mtupu peke yake!⁸⁰

81. Na wamechukua miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili ati iwape nguvu.⁸¹

82. Sivyo kabisa! Wataikataa hiyo ibada yao, na watakuwa ndio dhidi yao.⁸²

83. Kwani huoni ya kwamba tumewatuma mashet'ani kwa makafiri wawachochee

73 Na walikuwa makafiri duniani pindi wakisomewa Aya za Mwenyezi Mungu zenye kueleza wazi, wakizipuuza, na wakiwaambia Waumini kwa majivuno ya mali yao na watu wao: Nyinyi si kama sisi katika dunia. Sisi tuna cheo bora zaidi kuliko nyinyi, na hadhi zetu mabarazani ni kubwa zaidi. Hali kadhaalika itakuwa hali yetu Akhera mnayo iamini nyinyi.

74 Ingeli wafalia hawa makafiri wange waidhika kwa yaliyo wapata watu wengi walio watangulia. Wao walimkufuru Mwenyezi Mungu, na wakawa na cheo bora zaidi katika dunia, na starehe nyingi zaidi, na wakipendeza kuwaangalia. Na Mwenyezi Mungu akawateketeza kwa ukafiri wao - nao ni wengi. Na katika mabaki yao pana mafunzo kwa mwenye kuzingatia.

75 Ewe Mtume! Waambie hawa: Aliomo katika upotovu na ukafiri *Arrahmani*, Mwingi wa Rehema, humpa muhula, akamkunjulia umri, azidi ujabari wake na upotovu wake. Na makafiri huwakariria Waumini kauli kwa kusema: Kundi gani, baina yetu na nyinyi, lenye hadhi zaidi na bora katika mabaraza na majlisi? Mpaka watakapo ona yale walio ahidiwa, nayo ama kuadhibiwa na Waislamu duniani kwa kuuwawa na kutekwa, au kupata hizaya ya Siku ya Kiyama. Hapo tena watajijua kuwa hadhi yao ni duni, na msaada wao ni dhaifu.

76 Ama wenye kuamini Ishara za Mwenyezi Mungu, pindi wakizisikia tu wanazikubali. Na Mwenyezi Mungu huwazidishia tawfiki kwa vitendo vyao vizuri. Na vitendo vyema ni bora na vinadumu zaidi kwa Mwenyezi Mungu kwa malipo, na kuwa mwisho wake ni mwema.

77 Yafaa ustaajabu, ewe Mtume, huu mtindo wa anaye kanya Ishara za Mwenyezi Mungu. Mtu huyu amefitinika na dunia yake, akakanya kufufuliwa, akasema, kwa maskhara: Hakika Mwenyezi Mungu atanipa Akhera hiyo mnayo dai mali na wana nitafakhari nayo huko. Naye anadhani kuwa Akhera ni kama dunia, hukisiwa ya huko kama yalivyo huku. Amesahau kuwa huko ni malipo ya mema na mabaya, na kwamba kuzidiana huko ni kwa vitendo vyema.

78 Kwani huyo kafiri amejiua siri ya ghaibu, hata aieleze kwa ukweli? Na kwani amechukua ahadi kwa Mwenyezi Mungu kwa hayo hata awe na tamaa?

79 Basi na ayaache hayo anayo yazua. Kwani Sisi tunamhisabia uzushi wake, na atakuta adhabu yake imekunjuliwa muda mrefu kuliko anavyo fikiri.

80 Mwenyezi Mungu atampokonya yote anayo tafakhari nayo duniani, mali na wana; na atamtekeza. Na atakuja Akhera, peke yake, mtupu, hana mali wala mwana wala msaidizi.

81 Hao makafiri wamewafanya miungu mingine mbali mbali badala ya Mwenyezi Mungu wakaiabudu, ili wawe ndio waombezi wao Akhera.

82 Yawapasa waachilie mbali hayo wanayo yadhani. Hiyo miungu itakuja wapinga ibada yao na wataikanya. Na hiyo miungu itakuwa ndio makhasimu wa washirikina, na itaomba waadhibiwe.

kwa uchochezi?⁸³

84. Basi usiwafanyie haraka. Sisi tunawahisabia idadi ya siku zao.⁸⁴

85. Siku tutayo wakusanya wachamngu kuwapeleka kwa *Arrahmani* Mwingi wa Rehema kuwa ni wageni wake.⁸⁵

86. Na tukawachunga wakhalifu kuwapeleka Jahannamu hali ya kuwa wana kiu.⁸⁶

87. Hawatakuwa na mamlaka ya uombezi ila wale walio chukua ahadi kwa *Arrahmani* Mwingi wa Rehema.⁸⁷

88. Na wao ati husema kuwa *Arrahmani* Mwingi wa Rehema ana mwana!⁸⁸

89. Hakika mmeleta jambo la kuchusha mno!⁸⁹

90. Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo, na ardhi kupasuka, na milima kuanguka vipande vipande.⁹⁰

91. Kwa kudai kwao kuwa *Arrahmani* Mwingi wa Rehema ana mwana.⁹¹

92. Wala चाहिताजी *Arrahmani* Mwingi wa Rehema kuwa na mwana.⁹²

93. Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa *Arrahmani* Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa wake.⁹³

94. Yeye hakika amewadhibiti na amewahisabu sawa sawa.⁹⁴

95. Na kila mmoja katika wao atamfikia Siku ya Kiyama peke yake.⁹⁵

96. Hakika walio amini na wakatenda mema *Arrahmani* Mwingi wa Rehema atawajaalia mapenzi.⁹⁶

97. Na hakika tumeifanya nyepesi (Qur'ani) kwa ulimi wako, ili uwabashirie kwayo

83 Ewe Mtume! Hujui kama Sisi tumewapa madaraka mashetani juu ya makafiri - nao wamewazuga hawa makafiri - wanawaghuri na huwapeleka kwenye maasi waiache haki na wawafuate wao.

84 Basi ewe Mtume! Usiingie dhiki moyo wako kwa ukafiri wao, wala usiwatakie adhabu ya haraka. Kwani Sisi tunawawacha hivi duniani kwa muda wenye kiwango maalumu, na tunawadhibitia a'mali zao na madhambi yao, ili Akhera tuwahisabie.

85 Ewe Mtume! Itaje Siku tutapo wakusanya wachamngu kuwapeleka Peponi makundi kwa makundi yaliyo tukuzwa.

86 Na tutawachunga wakosefu kuwasukumia Jahannamu nao wamebanwa na kiu, kama wanavyo chungwa wanyama kwenda kwenye maji.

87 Na hapana ataye kuwa na mamlaka ya uombezi Siku hiyo yeyote isipo kuwa aliye pata ruhusa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ahadi aliyo mpa.

88 Washirikina, na Mayahudi, na Wakristo wamesema: Mwenyezi Mungu amejifanyia mwana kutokana na Malaika au kutokana na watu.

89 Enyi mlio sema hivyo, mmeleta jambo linalo chusha mno! Linalo chusha katika akili iliyo kaa sawa.

90 Mbingu zakaribia kupasuka kwa hayo, na ardhi kudidimia, na milima kuanguka mapande mapande.

91 Vituko hivyo vya mbingu, na ardhi, na milima, vyakaribia kutokea kwa sababu ya kumbandikiza Mwenyezi Mungu mwana!

92 Wala hayaingii akilini kuwa Mwenyezi Mungu awe na mwana; kwani kuthibiti kuwa na mwana Yeye inahitajia awe Yeye ni mwenye kuzuka, mwenye mwanzo na mwisho, na kuwa Yeye awe na haja ya mwana.

93 Hapana yeyote aliomo mbinguni na kwenye ardhi ila atamjia Mwenyezi Mungu, *Subhanahu*, Siku ya Kiyama hali naye ni mtumwa wake mwenye kuunyenyekeka Ungu wake.

94 Ujuzi wake umewaenea wao wote na wanayo yatenda. Hapana aliye fichikana kwake, wala chochote katika vitendo vyao.

95 Na wote hao watamjia Siku ya Kiyama hali ni wapweke, hawana wasaidizi wa kuwasaidia, wala wana, wala mali.

96 Hakika Waumini wenye kutenda mema Mwenyezi Mungu anawapenda, na anawapendezesha kwa watu.

wachamngu, na uwaonye kwayo watu wabishi.⁹⁷

98. Na kaumu ngapi tumezihiliki kabla yao. Je! Unawaona hata mmoja katika wao au unasikia hata mchakato wao?⁹⁸

97 Na hakika Sisi tumeifanya hii Qur'ani kuwa ni nyepesi, kwa lugha yako, ili kwa radhi ya Mwenyezi Mungu na neema zake uwape bishara nzuri wanao fuata amri zake, na wakaepuka makatazo yake. Na pia upate kuwaonya kwa hii Qur'ani wale wanao ipinga na wakakazana kuifanyia khasama, kuwa watapata ghadhabu za Mwenyezi Mungu na adhabu zake.

98 Ewe Mtume! Isikuhuzunishe inadi yao kwako. Kwani Mwenyezi Mungu amekwisha wahiliki kabla yao kaumu kadhaa wa kadhaa katika vizazi vilivyo tangulia. Wote wamemalizika. Huwaoni hata mmoja wao, wala huwasikii sauti yao.

Sura 20 - T'aha

Utangulizi

SURA HII ni ya Makka, isipo kuwa Aya mbili, nazo ni Aya 130 na 131. Hisabu ya Aya zake ni 135. Sura hii imeanza kwa harufi mbili za kuzindua juu ya muujiza wa Qur'ani, na kuwazindua wasikilizaji waisikilize. Baada ya harufi hizo mbili cheo cha Qur'ani kimetajwa, na utukufu wa hii Qur'ani ni utukufu wa Mwenye kuileta, naye ni Mwenyezi Mungu, *Subhanahu* wa Taa'la, Mmiliki mbingu na ardhi, Mwenye kujua siri, na kilicho fichikana kuliko siri. Kisha kimesimuliwa kisa cha Musa a.s. pamoja na Firauni, na vipi alipo anza kupewa utume Nabii Musa a.s. Na yametajwa maombi yake kutaka nduguye Harun a.s. awe msaidizi wake wa kumpa nguvu, tena vipi walivyo kutana na Firauni baada ya kitisho cha mkutano wake kwa ajili ya ujeuri wake. Na katika mintarafu ya haya Mwenyezi Mungu Mtukufu amebainisha kuzuka kwa Musa a.s.

Katika Sura hii pana majibizano baina ya Musa na Firauni, tena baina ya Musa a.s. na wachawi, na hali ya Musa ya kuogopa kushindwa mbele ya wachawi, na fimbo yake ilipo zimeza kamba zao, na tena mwisho vipi yalivyo ishia mambo ya wachawi na kuamini kwao, na Firauni kuwaadhibu. Kisha ikatajwa vipi Musa alivyo toka yeye na Wana wa Israili kutokana na Firauni, na vipi alivyo zama Firauni, naye alikuwa kawafuatia baada ya kupasuka bahari; na vipi Musa aliokoka akafika Jabal T'ur akawaacha watu wake ili ende kwenye mlima kuzungumza na Mola wake Mlezi. Na Msamaria akawafitini kwa kuwachochea waliabudu sanamu la ndama lililo undwa kwa dhahabu. Na ilikuwa ukipita upepo ndani yake hutoa sauti. Musa alikasirika kwa yaliyo tokea, akamkamata kichwa nduguye akimvutia kwake.

Kisha katika Sura hii tukufu yakatokea yaliyo msibu Msamaria. Mwenyezi Mungu Subhanahu amesimulia hadithi ya kuvuka katika hadithi za Musa na nyenginezo. Na mwisho wa Sura pana mausio mema juu ya Subira, na Usamehevu, na Sala. Kisha ikabainishwa kubwatika washirikina katika matakwa yao ya muujiza mwengine usio huu wa Qur'ani; na *Subhanahu* ameashiria hikima ya kuwatuma Mitume. Tena Sura hii tukufu imekhitimisha kwa kuashiria adhabu watakayo pata makafiri, na malipo mema watakayo pata Waumini.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. T'AHA!¹

2. Hatukukuteremshia Qur'ani ili upate mashaka.²

1 Mwenyezi Mungu Mtukufu ameanza Sura hii kwa harufi, nazo ni T'a na Ha, ili kupingana na makafiri wanao kanya, na kuwa kama ishara ya kwamba hii Qur'ani imeundwa kwa hizi hizi harufi mnazo zitumia katika kusema kwenu. Na juu ya hivyo nyinyi mmeajizika (yaani mmeshindwa, ndio likatokea hilo neno "Muujiza") kuleta Sura walau ndogo, au baadhi ya Aya zilizo mfano wa Qur'ani.

2 Ewe Mtume! Sisi hatukukufunulia wewe Qur'ani hii iwe ni sababu ya kukupa dhiki ya nafsi yako kwa kuwasikitikia hao wapuuzi kukupuza wewe.

3. Bali ni mawaidha kwa wenye kunyenyekea.³
4. Materemsho yatokayo kwa aliye umba ardhi na mbingu zilizo juu.⁴
5. *Arrahmani*, Mwingi wa Rehema, aliye tawala juu ya Kiti cha Enzi.⁵
6. Ni vyake vyote viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na viliomo baina yao, na viliomo chini ya ardhi.⁶
7. Na ukinyanyua sauti kwa kusema...basi hakika Yeye anajua siri na duni kuliko siri.⁷
8. Mwenyezi Mungu! Hapana mungu isipo kuwa Yeye. Yeye ana majina mazuri kabisa.⁸
9. Na je! Imekufikia hadithi ya Musa?⁹
10. Alipo uona moto, akawaambia watu wake: Ngojeni! Mimi nimeuona moto, huenda nikakuleteeni kijinga kutoka huo moto, au nikapata uongofu kwenye moto.¹⁰
11. Basi alipo ufikia akaitwa: Ewe Musa!¹¹
12. Hakika Mimi ndiye Mola wako Mlezi! Basi vua viatu vyako. Kwani upo katika bonde takatifu la T'uwa.¹²
13. Nami nimekuteua wewe; basi sikiliza unayo funuliwa.¹³
14. Hakika Mimi ndiye Mwenyezi Mungu. Hapana mungu ila Mimi tu. Basi niabudu Mimi, na ushike Sala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi.¹⁴
15. Hakika Saa itakuja bila ya shaka. Nimekaribia kuificha, ili kila nafsi ilipwe kwa iliyo yafanya.¹⁵
16. Kwa hivyo asikukengeushe nayo yule ambaye haiamini na akafuata pumbao lake ukaja kuhiliki.¹⁶

3 Lakini tumekuteremshia iwe ni kumbusho kwa mwenye kumkhofu Mwenyezi Mungu apate kumt'ii.

4 Hii Qur'ani umeteremshiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye uwezo, Muumba ardhi na mbingu zilizo nyanyuka juu.

5 Mtukufu wa rehema, ametawala sawa sawa juu ya Ufalme wake.

6 Ni wake Yeye tu, *Subhanahu*, ufalme wa mbinguni na viliomo humo, na wa ardhi na viliomo juu yake, na ufalme wa vilio baina ya hivyo, na maadeni na kheri nyenginezo zilizo fichikana chini ya ardhi.

7 Na kama uwezo wa Mwenyezi Mungu ulivyo kusanya kila kitu, kadhaalika ujuzi wake pia umekusanya kila kitu. Na ewe mtu, ukinyanyua sauti kwa kusema, basi Mwenyezi Mungu anajua. Kwani Yeye anajua unapo sema na mtu, na anajua unapo zungumza na nafsi yako.

8 Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, Mungu wa Pekee, Mwenye kustahiki kuabudiwa peke yake. Kwani Yeye amesifika kwa sifa za ukamilifu, naye ndiye Mwenye bora ya sifa.

9 Ewe Nabii! Unajua khabari za Musa na Firauni?

10 Pale Musa alipo uona moto katika safari yake ya usiku kutoka Madyana kwendea Misri, akamwambia mkewe na walio kuwa naye: Ngojeni hapa! Mimi nimeuona moto ule; natumai nitakupatieni kijinga cha moto kutoka kule mpate kuashia moto, au huko nitapata mtu wa kuniongoza njia.

11 Alipo fika huko, akasikia sauti yenye kutoka juu inamwita: Ewe Musa!

12 Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu, Mola wako Mlezi! Basi vua viatu vyako kwa hishima ya pahala hapa; kwani wewe upo katika bonde safi lenye baraka, nalo ni T'uwa.

13 Na Mimi Mwenyezi Mungu nimekuteua wewe kwa kukupa Utume. Basi sikiliza haya ninayo kufunulia uyajue na ukawafikishie watu wako.

14 Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu, Mungu wa Pekee, hapana wa kuabudiwa kwa haki isipo kuwa Mimi. Basi niamini Mimi, na niabudu Mimi, na dumu daima katika kuishika Sala ili uwe daima unanikumbuka.

15 Hakika Saa ndiyo miadi ya kukutana nami; nami miadi hiyo nimeificha kwa waja wangu, na nimewaonyesha ishara zake. Hiyo Saa itakuja bila ya shaka yoyote, na kila nafsi itahisabiwa kwa iliyo tenda.

16 Ewe Musa! Asikuachishe kuiamini Saa na kujitayarisha kwa ajili yake yule ambaye haisaidiki, na akafuata pumbao lake akahiliki.

17. Na nini hicho kilichomo mkononi mwako wa kulia, ewe Musa?¹⁷
18. Akasema: Hii ni fimbo yangu; naiegemea na ninawaangushia majani kondoo na mbuzi wangu. Tena inanifaa kwa matumizi mengine.¹⁸
19. Akasema: Itupe, ewe Musa!¹⁹
20. Akaitupa. Mara ikawa nyoka anaye kwenda mbio.²⁰
21. Akasema: Ikamate, wala usiogope! Tutairudisha hali yake ya kwanza.²¹
22. Na uambatishe mkono wako kwenye ubavu. Utatoka mweupe pasipo kuwa na madhara yoyote. Hiyo ni ishara nyengine.²²
23. Ili tukuonyeshe baadhi ya ishara zetu kubwa.²³
24. Nenda kwa Firauni; kwani hakika yeye amepindukia mipaka.²⁴
25. (Musa) akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu,²⁵
26. Na unifanyie nyepesi kazi yangu,²⁶
27. Na ulifungue fundo lililo katika ulimi wangu,²⁷
28. Wapate kufahamu maneno yangu.²⁸
29. Na nipe waziri katika watu wangu,²⁹
30. Harun, ndugu yangu.³⁰
31. Kwake yeye niongeze nguvu zangu.³¹
32. Na umshirikishe katika kazi yangu.³²
33. Ili tukutakase sana.³³
34. Na tukukumbuke sana.³⁴
35. Hakika Wewe unatuona.³⁵
36. Akasema: Hakika Umepewa maombi yako, ewe Musa!³⁶

17 Na nini hicho ulicho kamata kwa mkono wako wa kulia?

18 Musa akajibu: Hii ni fimbo yangu, najikongojea ninapo kwenda, na ninachungia kondoo na mbuzi wangu, na inanifaa kwa manufaa mengine, kama kuwatetea hayawani wangu.

19 Mwenyezi Mungu *Subhanahu* akamwambia Musa: Itupe hiyo fimbo chini kwenye ardhi.

20 Musa akaitupa; akashtuka kuiona imegeuka nyoka anakwenda!

21 Akamwogopa. Mwenyezi Mungu akamtuza kwa kumwambia: Mwokote wala usikhofu, kwani tutamrejsha hali yake kama ya kwanza.

22 Na ingiza mkono wako ndani ya mfuko wa nguo ukiambatisha na ubavu wako, utatoka mweupe safi bila ya maradhi. Na huo tumekufanyia ni muujiza wa pili wa Utume wako.

23 Ili tukuonyeshe baadhi ya miujiza yetu mikubwa iwe ni dalili ya ukweli wa Utume.

24 Nenda kwa Firauni umtake amuamini Mwenyezi Mungu Mmoja wa Pekee. Kwani yeye Firauni amepindukia mipaka kwa ukafiri wake na ujeuri wake.

25 Musa akamnyenyekea Mola wake Mlezi kwa kumwomba: Nikunjulie kifua changu, iniondoke ghadhabu, nitimize ujumbe wa Mola wangu Mlezi.

26 Na unisahilishie kazi yangu ili nipate kutimiza waajibu wangu.

27 Na likate fundo la ulimi wangu, nibainishe maneno,

28 Ili watu wafahamu vyema niyasemayo.

29 Na nijaalie mtu wa kuniunga mkono katika watu wangu,

30 Naye ni ndugu yangu Harun.

31 Anizidishe nguvu zangu.

32 Na umshirikishe nami katika kubeba mizigo ya ujumbe na kuifikisha.

33 Ili tukithirishe kukutakasa na yasiyo kuwa laiki yako.

34 Na tuyakariri majina yako mazuri kwa wingi.

35 Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe daima unatuangalia sisi, na unayashughulikia mambo yetu.

36 Mwenyezi Mungu akamwita Mtume wake, Musa, kwa kusema: Nimekwisha kukubalia uliyo yaomba, na hii ni zawadi tulio kutunukia wewe kwa hisani.

37. Na hakika tulikwisha kufanyia hisani mara nyengine.³⁷
38. Pale tulipo mfunulia mama yako yaliyo funuliwa,³⁸
39. Ya kuwa mtie katika kisanduku, na kisha kitie mtoni, na mto utamfikisha ufukweni. Atamchukua adui yangu naye ni adui yake. Na nimekutilia mapenzi yanayo tokana kwangu, na ili ulelewe machoni mwangu.³⁹
40. Dada yako alipo kwenda na akasema: Je! Nikujuulisheni mtu wa kuweza kumlea? Basi tukakurejesha kwa mama yako ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike. Na ulimuuwa mtu, nasi tukakuokoa katika dhiki, na tukakujaribu kwa majaribio mengi. Ukakaa miaka kwa watu wa Madyana. Kisha ukaja kama ilivyo kadiriwa, ewe Musa!⁴⁰
41. Na nimekuteuwa kwa ajili ya nafsi yangu.⁴¹
42. Nenda, wewe na ndugu yako, pamoja na ishara zangu, wala msichoke kunikumbuka.⁴²
43. Nendeni kwa Firauni. Hakika yeye amepindukia mipaka.⁴³
44. Mwambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa.⁴⁴
45. Wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tunaogopa asije akapindukia mipaka juu yetu au kufanya jeuri.⁴⁵
46. Akasema: MsioCOPE! Hakika Mimi ni pamoja nanyi. Nasikia na ninaona.⁴⁶
47. Basi mwendeeni, na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi! Basi waache Wana wa Israili watoke nasi, wala usiwaadhibu. Sisi tumekuletea ishara itokayo kwa Mola wako Mlezi. Na amani itakuwa juu ya aliye fuata uwongofu.⁴⁷
48. Hakika tumefunuliwa sisi kwamba hapana shaka adhabu itamsibu anaye kadhibisha

37 Na Sisi tumewahi zamani kukufadhili wewe kwa hisani bila ya kuomba.

38 Tulipo mwongoza mama yako kwa uwongozi wenye nafuu katika maisha yako.

39 Tulimuamrisha akuweke, na hali wewe ni mtoto mchanga wa kunyonya, katika kisanduku, na kisha hicho kisanduku akitie katika mto, ili usije kuuliwa na Firauni, pale alipo kuwa anawauwa watoto wote wanaume wa Banu Israili. Tukayafanya maji ya mto yachukue kisanduku kile mpaka ufukweni. Kwa mujibu wa mipango yetu Firauni, adui yangu na wako, akakichukua kile kisanduku. Nami nikakupapa mapenzi ya rehema na ulinzi, ukapendwa na kila aliye kuona. Ukapata malezi mazuri yaliyo bora chini ya ulinzi wangu.

40 Ewe Musa! Jua ya kwamba zamani Sisi tulikwisha kufanyia hisani pale dada yako alipo kuwa anakwenda akiangalia hali yako ulipo kuwa katika jumba la Firauni, na akawaona wanakutafutia mtu wa kukunyonyesha. Ni yeye aliye waongoza kwa mama yako, nasi tukakurejesha kwake apate kufurahi kukuona uhai na umerejea kwake, na asite huzuni na kilio. Na ulipo kua, na ukamuuwa mtu katika kaumu ya Firauni bila ya kukusudia, tukakuvua kutokana na dhiki iliyo kupata, na tukakusalimisha na shari yao. Ukenda mpaka Madyana na huko ukakaa miaka kadhaa wa kadhaa, kisha ukatoka Madyana ukarejea kwa muda tulio kukadiria kwa ujumbe wako.

41 Na nikakuteua kukupa Wahyi (Ufunuo) na kubeba Utume wangu.

42 Nenda, wewe na nduguyo, nanyi mkisaidiwa na miujiza yangu yenye kuashiria Unabii na Utume, wala msidhoofike katika kutimiza Ujumbe wangu, wala msighafilike kunikumbuka na kuniomba msaada.

43 Nenda pamoja na duguyo Harun kwa Firauni. Hakika huyo amepindukia mipaka katika ukafiri wake na jeuri zake.

44 Mtakeni kwa upole na ulaini aniamini Mimi kwa kutaraji asaa akakumbuka Imani aliyio isahau, na akaogopa matokeo ya ukafiri wake na ujeuri wake.

45 Musa na Harun wakanyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tunaogopa huyu Firauni asituvamie kwa madhara, na akapindukia mpaka katika uovu.

46 Mwenyezi Mungu akawapoza kwa kusema: Msimkhofu Firauni; kwani Mimi ni pamoja nanyi kukuangalieni na kukulindeneni, nayasikia ayasemayo, na nayaona ayatendayo. Sitomwachia kukudhuruni.

47 Nendeni kwa Firauni, na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume tulio tumwa kwako na Mola wako Mlezi. Tumekuja kukutaka umuamini Yeye, na uwaache Wana wa Israili watoke utumwani na adhabuni. Na sisi tumekuletea muujiza kutokana na Mwenyezi Mungu kuwa ni ushahidi wa ukweli wa haya tunayo kuitia, na mwenye kuufuata uwongofu atasalimika na adhabu ya Mwenyezi Mungu na kughadhibika kwake.

na akapuuza.⁴⁸

49. (Firauni) akasema: Basi Mola wenu Mlezi ni nani, ewe Musa?⁴⁹

50. Akasema: Mola wetu Mlezi ni yule aliye kipa kila kitu umbo lake, kisha akakiongoa.⁵⁰

51. Akasema: Nini hali ya karne za kwanza?⁵¹

52. Akasema: Ilimu yake iko kwa Mola wangu Mlezi katika Kitabu. Mola wangu Mlezi hapotei wala hasahau.⁵²

53. Ambaye amekufanyieni ardhi kuwa tandiko, na akakupitishieni humo njia, na akakuteremshieni kutoka mbinguni maji. Na kwa hayo tukatoa namna mbali mbali za mimea.⁵³

54. Kuleni, na mchunge wanyama wenu. Hakika katika hayo zipo ishara kwa wenye akili.⁵⁴

55. Kutokana nayo (ardhi) tumekuumbeni, na humo tunakurudisheni, na kutoka humo tutakutoeni mara nyengine.⁵⁵

56. Na hakika tulimwonyesha ishara zetu zote. Lakini alikadhibisha na akakataa.⁵⁶

57. Akasema: Ewe Musa! Hivyo umetujia kututoa katika nchi yetu kwa uchawi wako?⁵⁷

58. Basi sisi hakika tutakueletea uchawi kama huo. Basi weka miadi baina yetu na wewe, ambayo tusiivunje sisi wala wewe, mahali patapo kuwa sawa.⁵⁸

59. Akasema: Miadi yenu ni siku ya Sikukuu; na watu wakusanywe kabla ya adhuhuri.⁵⁹

48 Na hakika Mwenyezi Mungu ametufunulia sisi kuwa adhabu yake kali itamshukia anaye tukadhibisha, na akapuuza wito wetu.

49 Firauni kwa ujeuri wake na ujabari wake akasema: Ewe Musa! Ni nani huyo Mola wenu Mlezi?

50 Musa akamjibu: Mola wetu Mlezi ni yule aliye kipa neema ya umbo kila kilicho umbwa, akakiumba kwa sura aliyo ipenda Yeye *Subhanahu*, na akakielekeza kwa alivyo kiumba. (*Tazama* Maelezo 20:50)

51 Firauni akasema: Je, nini hali ya karne za zamani, na yaliyo pitikana huko?

52 Musa akasema: Ujuzi wa karne hizo uko kwa Mola wangu Mlezi peke yake. Hayo yamedhibitiwa katika madaftari ya vitendo vyao. Hapana kitendo kinacho mpootea asikijue, wala Yeye hasahau.

53 Yeye huyo ndiye Mungu Mwenye kuwafadhili waja wake kwa kuwaumba na kuwalinda. Amekutengenezeni ardhi, akaikunjua kwa uwezo wake, na akakupasulieni njia mnazo pitia, na akakuteremshieni mvua zinazo leta mito, na Yeye *Subhanahu* akatoa namna mbali mbali za mimea, inayo khitalifiana kwa rangi, na utamu, na manufaa. Mengine myeupe, mengine myeusi, myengine mitamu na mengine michungu.

54 Naye *Subhanahu* amewaelekeza waja wake wanufaike kwa mimea aliyo watolea, kwa kula na kulishia mifugo yao na kama hayo. Na akataja kuwa katika kuumba huku, na kuanzisha huku, na kutumia huku, ni dalili zilizo wazi za kumwongoa mwenye akili afikie Imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu na kuamini Mitume wake.

55 Na kutokana na udongo wa ardhi hii ndio Mwenyezi Mungu amemuumba Adam na dhuriya zake. Na humo ndio anawarudisha baada ya kufa kwa ajili ya kusitiri miili yao. Na kutoka humo atawatoa tena kuwafufua na kuwalipa kwa waliyo yatenda.

56 Na hakika Sisi kwa kupitia kwa Musa tulimwonyesha Firauni miujiza ya dhahiri ya kuunga mkono Ujumbe wa Musa na ukweli wake kwa yote aliyo simulia kutokana na Mwenyezi Mungu na athari ya uwezo wake. Juu ya hayo Firauni alishikilia ukafiri wake, akayakadhibisha yote hayo, na akakataa kuyaamini.

57 Firauni akamwambia Musa: Je, umetujia upate kututoa katika nchi yetu ipate kuwa mikononi mwa watu wako kwa uchawi wako ulio ulia watu?

58 Basi sisi tutavunja huo uchawi wako. Weka miadi baina yetu na wewe, tukutane, wala tusikhitalifiane.

59 Musa akawajibu: Miadi yetu ni siku ya Idi yenu mnapo jipamba, na watu wakusanyike kabla ya adhuhuri siku hiyo, waone yatayo kuwa baina yetu na nyinyi.

60. Basi Firauni akarudi na akatengeneza hila yake, kisha akaja.⁶⁰
61. Musa akamwambia: Ole wenu! Msimzulie Mwenyezi Mungu uwongo, asije akakufutilieni mbali kwa adhabu. Na mwenye kuzua lazima ashindwe!⁶¹
62. Basi wakazozana kwa shauri yao wenyewe kwa wenyewe, na wakanong'ona kwa siri.⁶²
63. Wakasema: Hakika hawa wawili ni wachawi, wanataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wao, na waondoe mila zenu zilizo bora kabisa.⁶³
64. Kwa hivyo kusanyeni hila zenu zote, kisha mfike kwa kujipanga safu, na kwa yakini atafuzu kweli kweli leo atakaye shinda.⁶⁴
65. Wakasema: Ewe Musa! Je! Utatupa wewe, au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa?⁶⁵
66. Akasema: Bali tupeni nyinyi! Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio.⁶⁶
67. Basi Musa akaingia khofu nafsi yake.⁶⁷
68. Tukasema: Usikhofu! Hakika wewe ndiye utakaye shinda.⁶⁸
69. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyo viunda. Hakika walivyo unda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo.⁶⁹
70. Basi wachawi wakaangushwa wanasujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa Harun na Musa!⁷⁰
71. (Firauni) akasema: Oh! Mnamuamini kabla sijakupeni ruhusa? Hakika yeye ndiye mkubwa wenu aliye kufundisheni uchawi. Basi kwa yakini nitakukatani mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakutundikeni misalabani katika vigogo vya mitende, na hapo kwa yakini mtajua ni nani katika sisi aliye mkali wa kuadhibu na

60 Firauni akaondoka na akayashughulikia mambo mwenyewe. Akakusanya mipango yake, na wakuu wa wachawi, na zana za uchawi. Kisha akahudhuria na yote hayo kwa mujibu wa miadi.

61 Musa akawaambia kuwahadharisha maangamizo ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake, na akawakataza wasizue uwongo, kwa kumdaia ungu Firauni, na kuwakadhibisha Mitume wa Mwenyezi Mungu, na kuikataa miujiza. Na akawatisha kwamba Mwenyezi Mungu atawapatiliza kwa adhabu wakiendelea na hayo, na akatilia mkazo sana khasara ya mwenye kumzulia uwongo Mwenyezi Mungu.

62 Wakatishika na maonyo ya Musa, wakaingia kusemezana wao kwa kwao wakivutana, na kila mmoja akitoa maoni yake juu ya aliye yasema Musa.

63 Wakawafikiana kwamba Musa na Harun ni wachawi ambao wanafanya hila kutaka kuwatoa katika nchi yao, kwa kuwapokonya madaraka, yatoke mikononi mwao. Na hayo ni kwa uchawi, ili Wana wa Israili wapate ushindi. Na wawaharibie watu wa Firauni imani yao wanayo iona kuwa ni nzuri!

64 Basi fanyeni njama zenu muwafikiane kitu kimoja cha kumfanyia Musa, kisha mkusanye wateuliwa, ili watazamaji waingiwe na kitisho kwa heba yao. Atakaye fuzu leo basi ndio kashinda kweli.

65 Wachawi walimkabili Musa kwa rai moja, na wakamkharisha kwa majivuno na kiburi, waanze wao au aanze yeye kuonyesha ubingwa wake.

66 Musa akasema: Bali anzeni nyinyi! Basi wakazitupa kamba zao na fimbo zao. Zikamdhihirikia Musa, kwa uchawi, kuwa zimegeuka nyoka zinakwenda.

67 Musa akaingiwa na khofu kwa aliye yaona kwa kuzugwa na uchawi, na kuona huenda watu wakadanganyika kwa uchawi wakadhani ni muujiza.

68 Mwenyezi Mungu akamdiriki kwa upole, akamwambia: Usiogope kitu. Wewe utaushinda tu leo huu upotovu wao.

69 Itupe hiyo fimbo uliyo nayo mkononi mwako wa kulia ivimeze hivyo walivyo vizua kwa uchawi. Kwani hayo waliyo yaunda ni mazonge tu ya uchawi, na hakika mchawi popote alipo hawezi kufuzu.

70 Musa akaitupa fimbo yake, na hapo hakika ikageuka kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ikawa joka kubwa la kutisha. Likavimeza vyote walivyo unda wao. Wachawi walipo uona muujiza huu mbio mbio wakasujudu kwa kuyakinika na ukweli wa Musa, huku wakisema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu Mmoja wa Pekee, Mola Mlezi wa Harun na Musa, Mola Mlezi wa kila kitu.

kuiendeleza adhabu yake.⁷¹

72. Wakasema: Hatutokukhiari wewe kuliko ishara waziwazi zilizo tujia, na kuliko yule aliye tuumba. Basi hukumu utavyo hukumu; kwani wewe unahukumu haya ya maisha ya duniani tu.⁷²

73. Hakika sisi tumemuamini Mola wetu Mlezi ili atusamehe makosa yetu na uchawi ulio tulazimisha kuufanya. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mbora na Mwenye kudumu zaidi.⁷³

74. Hakika ataye mjia Mola wake Mlezi naye ni mkhalifu, basi kwa yakini, yake huyo ni Jahannamu. Hafi humo wala haishi.⁷⁴

75. Na atakaye mjia naye ni Muumini aliye tenda mema, basi hao ndio wenye vyeo vya juu.⁷⁵

76. Bustani za milele zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na hayo ni malipo ya mwenye kujitakasa.⁷⁶

77. Na tulimfunulia Musa: Toka usiku na waja wangu, na uwapigie njia kavu baharini. Usikhofu kukamatwa, wala usiogope.⁷⁷

78. Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake. Basi kiliwafudikiza humo baharini kilicho wafudikiza.⁷⁸

79. Na Firauni aliwapoteza watu wake wala hakuwaongoa.⁷⁹

80. Enyi Wana wa Israili! Hakika tulikuokoeni na adui yenu, na tukakuahidini upande

71 Firauni akasema: Vipi mnamuamini huyu bila ya ruhusa yangu? Hakika huyu ndiye mkubwa wenu aliye kufunzeni uchawi, wala kitendo chake hichi si muujiza kama mnavyo dhani! Akawatishia kwa kusema: Kwa yakini nitaikata mikono yenu na miguu yenu mbali mbali, mkono wa kulia kwa mguu wa kushoto n.k. Na hakika nitakubandikeni misalabani kwenye vigogo vya mitende. Na hapo mtajua ni mungu gani kati yetu aliye mkali zaidi na kudumu zaidi katika mateso - mimi au mungu wa Musa?

72 Wachawi wakasimama imara juu ya Imani yao, na wakajibu vitisho vya Firauni kwa kauli yao: Sisi hatuendelei na kubakia nawe katika ukafiri baada ya kwisha tubainikia yaliyo ya kweli katika muujiza wa Musa. Wala sisi hatutakukhiari wewe kuliko Mungu wa Musa ambaye ndiye aliye tuumba. Basi wewe tenda utakayo yatenda! Madaraka yako hayapindikii maisha haya mafupi.

73 Kwani hakika sisi ni wenye kusimama juu ya Imani kumuamini Mola wetu Mlezi wa Haki, ili atufutie madhambi yetu yaliyo pita, na atusamehe huku kushughulikia uchawi ulio tulazimisha tujifunze na tuufanye! Na Mola wetu Mlezi ni Mbora wa malipo kuliko wewe, akit'iwiwa; na ufalme wake na uwezo wake kulipa unadumu zaidi kuliko wako.

74 Hakika anaye kufa katika ukafiri akakutana na Mwenyezi Mungu hali naye ni mkhalifu basi malipo yake ni Jahannamu. Humo hafi, akapumzika na adhabu; wala hawi hai wa maisha ya kustarehe na neema.

75 Na mwenye kukutana na Mola wake Mlezi naye yumo katika Imani na a'mali njema, basi huyo atakuwa na vyeo vya juu.

76 Vyeo hivyo ni Bustani za Peponi za kudumu katika neema. Baina ya miti yake inapita mito, na humo watadumu milele. Hayo ni malipo ya mwenye kuitakasa nafsi yake na ukafiri kwa kuijaza Imani, na ut'iifu baada ya ukafiri na maasi.

77 Tena vikapishana vituko baina ya Firauni na Musa. Mwenyezi Mungu akampa Wahyi (ufunuo) Mtume wake, Musa, atoke Misri na Wana wa Israil, wakati wa usiku. Na aipige bahari kwa fimbo yake, utatokea muujiza mwingine, nao ni kufunguka njia kavu baharini. Naye akamtuliza asiingiwe na khofu kuwa atakamatwa na Firauni, au kuwa atazama katika maji.

78 Musa akafanya kama alivyo muamrisha Mwenyezi Mungu. Akatoka Firauni na askari wake nyuma yake, akawakuta kwenye bahari. Akenda nyuma yao kwenye njia iliyo funguka baharini kwa ajili ya Musa na kaumu yake. Na hapo ukatokea muujiza; nao ni maji kumfudikiza Firauni na kaumu yake, wakazama wote!

79 Hivi ndivyo Firauni alivyo potea yeye na watu wake wakaacha Haki, wakateketea wote!

wa kulia wa mlima. Na tulikuteremshieni Manna na Salwa.⁸⁰

81. Kuleni katika vitu vizuri hivyo tulivyo kuruzukuni, wala msiruke mipaka katika hayo, isije ikakushukieni ghadhabu yangu. Na inaye mshukia ghadhabu yangu basi huyo ameangamia.⁸¹

82. Na hakika Mimi ni Mwingi wa Kusamehe kwa anaye tubia, na akaamini, na akatenda mema, tena akaongoka.⁸²

83. Na nini kilicho kutia haraka ukawaacha watu wako, ewe Musa?⁸³

84. Akasema: Hao wapo nyuma yangu wananifuatia. Na nimefanya haraka kukujia, Mola wangu Mlezi, ili uridhike.⁸⁴

85. (Mwenyezi Mungu) akasema: Sisi tumewatia mtihani watu wako baada yako, na Msamaria amewapoteza.⁸⁵

86. Musa akarudi kwa watu wake kwa ghadhabu na kusikitika. Akasema: Enyi watu wangu! Kwani Mola wenu Mlezi hakukuahidini ahadi nzuri? Je, umekuwa muda mrefu kwenu au mmetaka ikushukieni ghadhabu ya Mola wenu Mlezi, ndio maana mkavunja miadi yangu?⁸⁶

87. Wakasema: Sisi hatukuvunja miadi yako kwa khiari yetu, lakini tulibebeshwa mizigo ya mapambo ya watu, basi tukaitupa. Na hivyo ndivyo alivyo toa shauri Msamaria.⁸⁷

88. Na akawaundia ndama, kiwiliwili chenye sauti. Na wakasema: Huyu ndiye mungu wenu, na mungu wa Musa, lakini alisahau.⁸⁸

80 Enyi Wana wa Israili! Sisi tulikuokoeni na adui yenu, Firauni, na tukakuahidini kuokoka kwa ulimi wa Musa kuwa mtafika salama mpaka kwenye kando ya mlima. Na tulikuteremshieni Manna na Salwa, chakula kizuri, cha tam-tam na nyama ya ndege nono.

81 Kuleni vitu hivi vizuri tulivyo kuruzukuni bila ya taabu yoyote kwenu. Wala msidhulumu, wala msiingie kumuasi Mwenyezi Mungu katika maisha haya ya starehe, isije kukuteremkieni ghadhabu yangu. Kwani anaye teremkiwa na ghadhabu yangu huporomoka katika matabaka ya chini kabisa ya mateso ya Mwenyezi Mungu.

82 Na hakika Mimi ni Mtukufu wa Kusamehe kwa anaye acha ukafiri wake, na akatengeneza Imani, na akatenda yaliyo mema, na akadumu juu ya hayo mpaka akakutana na Mwenyezi Mungu.

83 Musa aliwatangulia watu wake kwenda mlimani, apate kuzungumza na Mola wake Mlezi. Mwenyezi Mungu akamuuliza sababu ya kufanya kwake haraka kufika mbele kabla ya kaumu yake.

84 Musa akasema: Hakika watu wangu wapo karibu nami, watanikuta. Ewe Mola wangu Mlezi! Mimi nimewatangulia ili kutaka kukuridhisha Wewe.

85 Mwenyezi Mungu akamwambia: Sisi tumewafanyia mtihani watu wako baada ya wewe kuwawacha. Wakaingia katika fitna; Msamaria amewapotoa!

86 Musa akawarejea watu wake naye kaghadhibika sana, na huzuni ya uchungu. Akawasemeza watu wake kwa hamaki: Mola wenu Mlezi alikuahidini kuwa atakuokoeni na atakuongoeni, kwa kuitereemsha Taurati na kupata ushindi kwa kuingia nchi takatifu. Haujapita muda mrefu wa ahadi ila nyinyi mmekwisha saha ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyu kupeni. Kwa kitendo chenu kiovu hichi mnataka ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ikuteremkieni kwa maasi yenu aliyu kuhadharisheni nayo? Mmesahau ahadi yenu mliyo nipa kuwa mtafuata mwendo wangu, na mtafuata nyayo zangu?

87 Watu wa Musa wakasema kwa kutafuta udhuru: Hatukwenda kinyume na ahadi yako kwa khiari yetu. Lakini tulipo toka Misri tulibebeshwa mizigo ya mapambo ya watu. Kisha tukaona - kwa uzito wake kwetu - tuepukane nayo. Msamaria akawasha moto katika shimo, tukaitupa hiyo mizigo. Na kadhaalika Msamaria naye katupa vyombo alivyo kuwa navyo.

88 Basi Msamaria akawaundia ndama aliye na mwili wa dhahabu, ukipita upepo ndani yake, hutoa sauti, husikilizana kama mlio wa ng'ombe, ili udanganyifu utimie. Akawaita wamuabudu na wao wakamwitikia. Akasema yeye na wafwasi wake: Huyu ndiye mungu wenu, na ndiye mungu wa Musa. Akasahau Msamaria kuwa ni wepesi mtu, akizingatia na kutafuta dalili, kufahamu kuwa ndama hawezi kuwa mungu.

89. Je! Hawakuona kuwa hakuwarudishia neno, wala hakuweza kuwadhuru wala kuwafaa?⁸⁹
90. Na hakika Harun alikwisha waambia kabla yake: Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmetiwa mtihanini tu kwa kitu hiki. Na kwa yakini Mola wenu Mlezi ni *Arrahmani*, Mwingi wa Rehema. Basi nifuateni mimi, na t'iini amri yangu!⁹⁰
91. Wakasema: Hatutaacha kumuabudu mpaka Musa atapo rejea kwetu.⁹¹
92. (Musa) akasema: Ewe Harun! Ni nini kilicho kuzuia, ulipo waona wamepotea,⁹²
93. Hata usinifuute? Je, umeasi amri yangu?⁹³
94. Akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Usinishike ndevu zangu, wala kichwa changu. Kwa hakika naliogopa usije sema: Umewafarikisha Wana wa Israil, na hukungojea kauli yangu.⁹⁴
95. (Musa) akasema: Ewe Msamaria! Unataka nini?⁹⁵
96. Akasema: Niliona wasiyo yaona wao, nikashika gao katika unyao wa Mtume. Kisha nikalitupa. Na hivi ndivyo ilivyo nielekeza nafsi yangu.⁹⁶
97. (Musa) akasema: Basi ondoka! Na kwa yakini utakuwa katika maisha ukisema: Usiniguse. Na hakika una ahadi kwako isiyo vunjwa. Na mtazame huyo mungu wako uliye endelea kumuabudu - Sisi kwa hakika tutamchoma moto, kisha tutamtawanya baharini atawanyike.⁹⁷
98. Hakika Mungu wenu ni Allah, Mwenyezi Mungu, tu. Hapana Mungu isipo kuwa Yeye. Ujuzi wake umeenea kila kitu.⁹⁸

89 Macho yaliingia upofu yalipo zingatia kuwa huyu ndama ni mungu! Hawaoni kwani hawarejezei kauli yao? Wala hawezi kuwaondolea madhara yoyote? Wala kuwaletea manufaa yoyote?

90 Na Harun alikuwa pamoja nao ilipo tokea fitna hii. Naye kabla ya kurejea Musa a.s. alikwisha waambia: Enyi watu wangu! Nyinyi mmeingia katika fitna ya Msamaria kwa upotovu huu! Hakika Mungu wenu wa Haki ni Mwenyezi Mungu, *Arrahman*, Mwingi wa Rehema, wala hana mwengine. Nifuateni mimi kwa haya ninayo kunasihini, na ishikeni rai yangu kwa kuachilia mbali upotovu huu.

91 Wakasema: Sisi tutaendelea kumuabudu huyu ndama mpaka atakapo rejea Musa kwetu!

92 Musa kwa kuathirika na aliyo yajua na kuyaona ya watu wake, alisema: Ewe Harun! Sababu gani iliyo kukataza hata usiwazuie na upotovu ulipo kwisha waona wameuingia?

93 Na usisimame msimamo wangu kwa kuwanasihii kama nilivyo chukua ahadi kwako? Hukunifuata katika ahadi niliyo ahidiana nawe, au umevunja amri yangu?

94 Harun akamwambia Musa: Ewe mwana wa mama yangu! Usinichukulie papara kwa hasira zako, wala usizishike ndevu zangu na kichwa changu. Hakika mimi nilikihofu lau ningeli wafanyia ukali, wakafarikiana makundi na mapande usije ukaniambia: Umewagawanya Wana wa Israil, wala hukuyafuata niliyo chukua ahadi kwako.

95 Musa a.s. akamwambia Msamaria: Jambo hili jambo gani la khatari ambalo laonekana ni balaa ulilo lizua?

96 Msamaria akamwambia Musa: Nimejua ustadi wa ufundi na mbinu zake wasizo zijua Wana wa Israil; nikawaundia sanamu la ndama lenye kutoa sauti, na nikachukua sehemu ya Taurati nikaitia ndani ya ndama, kuwazuga watu. Basi ndio hivyo, nafsi yangu imenizaini nifanye hayo niliyo yafanya.

97 Musa akamwambia Msamaria: Tokana nasi, na uwe mbali nasi. Na jaza yako duniani uwe unatanga tanga ovyo, na watu wakikukimbia, mpaka usiwe na makhusiano na yeyote, na asiwepo ndudu ya mtu kukukaribia, wala wewe usimkaribie mtu. Na hakika adhabu yako kesho Akhera umewekewa kwa ahadi huwezi kuikimbia! Musa tena akimbeua huyo mungu wake kwa kusema: Tazama sasa nini tunalo mfanyia huyu mungu wako ulio kaa wewe ukimuabudu, na kwa sababu yake ukawafitini watu! Tutamuunguza, na kisha tutamtawanya baharini apotelee mbali!

98 Musa akaingia kutimiza aliyo yasema, na kisha baada ya mazingatio hayo aliwaelekea Wana wa Israili kuwaambia: Hakika Mungu wenu ni Mmoja. Yeye ndiye ambaye hapana anaye abudiwa kwa haki isipo kuwa Yeye. Na ujuzi wake umeenea kila kitu kilicho kuwa na kitakacho kuwa.

99. Namna hivi tunakuhadithia katika khabari za yaliyo tangulia. Na hakika tumekuletea kutoka kwetu mawaidha ya kukumbukwa.⁹⁹
100. Atakaye jitenga nayo, basi kwa yakini Siku ya Kiyama atabeba mzigo.¹⁰⁰
101. Wadumu humo. Na ni mzigo muovu kwao kuubeba Siku ya Kiyama!¹⁰¹
102. Siku litakapo pulizwa barugumu, na tukawakusanya wakhalifu Siku hiyo, hali macho yao ya kibuluu.¹⁰²
103. Watanong'onezana wao kwa wao: Hamkukaa ila siku kumi tu.¹⁰³
104. Sisi tunajua zaidi watakayo yasema, atakapo sema mbora wao katika mwendo: Nyinyi hamkukaa ila siku moja tu.¹⁰⁴
105. Na wanakuuliza khabari za milima. Waambie: Mola wangu Mlezi ataivuruga vuruga.¹⁰⁵
106. Na ataiacha tambarare, uwanda.¹⁰⁶
107. Hutaona humo mdidimio wala muinuko.¹⁰⁷
108. Siku hiyo watamfuata muitaji asiye na upotofu. Na sauti zote zitamnyenyekea *Arrahmani* Mwingi wa Rehema. Basi husikii ila mchakato na mning'ono.¹⁰⁸
109. Siku hiyo uombezi haufai kitu, ila wa aliye mruhusu *Arrahmani* Mwingi wa Rehema na akamridhia kusema.¹⁰⁹
110. Yeye anajua yaliyo mbele yao, na yaliyo nyuma yao. Wala wao hawawezi kumjua Yeye vilivyo.¹¹⁰

99 Ewe Mtume! Kama tulivyo kusimulia khabari za Musa, tunakupa khabari za kweli za kaumu zilizo tangulia. Na Sisi tumekuteremshia wewe Kitabu kutoka kwetu, ndani yake yamo mawaidha kwako na kwa umma wako, ya kukufaeni katika Dini yenu na dunia yenu.

100 Mwenye kuacha kukiamini Kitabu hicho na kufuata uwongofu wake, basi amepotea katika maisha yake, na Siku ya Kiyama atakuja naye amebeba madhambi ya aliyo yatenda, na atalipwa kwa adhabu kali.

101 Na atadumu katika adhabu hii, na ni mzigo muovu kweli huo Siku ya Kiyama.

102 Ewe Mtume! Watajia umma wako Siku ambayo tutawaamrisha Malaika walipulize baragumu la kuwafufua watu kutoka makaburini, na kuwaita hapo pa mkutano, na tutapo wachunga wakhalifu kwendea ufundoni na nyuso zao rangi ya buluu kwa khofu na kitisho.

103 Wakinong'onezana wao kwa wao katika udhalili na kubabaika jinsi walivyo ona maisha ya dunia ni mafupi, hata waone kama kwamba hawajapata kustarehe nayo, na wala hawakukaa humo duniani ila siku kumi tu.

104 Wala si kama hiyo minong'ono yao ndiyo haisikilizani, kwani Sisi tunajua vyema wao wananong'onezana nini, na tunayajua vyema wanayo yasema wale walio kuwa mahodari zaidi kulinganisha hisiya zao kwa dunia, kuwa hayo maisha ya duniani ni kama kwamba hayakutimia hata siku moja.

105 Ewe Mtume! Wanakuuliza hao wanao kanya kufufuliwa, nini hali ya milima Siku ya Kiyama hiyo unayo itaja? Wajibu: Mwenyezi Mungu ataivuruga kama mchanga, kisha ataipeperusha kwa upepo kama vumbi!

106 Na pahala pao baada ya kwisha vurugika milima patakuwa sawa sawa laini.

107 Hutoona kwenye ardhii kudidimia wala kunyanyuka, kama kwamba haikupata kukaliwa kabla yake.

108 Siku ya Kiyama watu wakisha toka makaburini, watamfuata mwenye kuwaita mpaka pahala pa mkutano nao wamesalimu amri. Hawezi yeyote kati yao kuelekea kulia wala kushoto. Sauti zote zimenyenyekea kwa utulivu na kitisho kwa utukufu wake *Arrahmani*, Mwingi wa Rehema. Basi husikii ila sauti ya chini kabisa ya mning'ono.

109 Siku hiyo hapana uombezi unao faa kitu, ila wa aliye pata hishima ya Mwenyezi Mungu kwa kuruhusiwa naye na kuridhiwa aseme. Na hapana uombezi wa yeyote utao faa ila wa aliye pata ruhusa ya Mwenyezi Mungu kuombea, na akawa ni Muumini, na Mwenyezi Mungu akaridhia kauli yake kwa Tawhidi na Imani.

110 Na Mwenyezi Mungu, aliye tukuka shani yake, anayajua mambo yao waliyo yakadimisha katika dunia yao na waliyo yaakhirisha. Yeye *Subhanahu* anawapangia mambo yao kwa mujibu wa ujuzi wake.

- 111.** Na zitadhalilika nyuso mbele ya Aliye Hai Milele, Mwangalizi Mkuu. Na atakuwa ameharibikiwa mwenye kubeba dhulma.¹¹¹
- 112.** Na anaye tenda mema, naye ni Muumini, basi hatakhofu kudhulumiwa wala kupunjwa.¹¹²
- 113.** Na namna hivi tumeiteremsha Qur'ani kwa Kiarabu, na tumekariri humo maonyo ili wapate kuogopa na kujilinda na iwalettee makumbusho.¹¹³
- 114.** Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki. Wala usiifanyie haraka hii Qur'ani, kabla haujamalizika ufunuo wake. Na sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie ilimu.¹¹⁴
- 115.** Na hapo zamani tuliagana na Adam, lakini alisahau, wala hatukuona kwake azma kubwa.¹¹⁵
- 116.** Na tulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam! Wakasujudu, isipo kuwa Iblisi, alikataa.¹¹⁶
- 117.** Tukasema: Ewe Adam! Hakika huyu ni adui yako na wa mkeo. Basi asikutoeni katika Bustani hii, mkaingia mashakani.¹¹⁷
- 118.** Hakika humo hutakuwa na njaa wala hutakuwa uchi.¹¹⁸
- 119.** Na hakika hutapata kiu humo wala hutapata joto.¹¹⁹
- 120.** Lakini Shet'ani alimtia wasiwasi, akamwambia: Ewe Adam! Nikujuulishe mti wa kuishi milele na ufalme usio koma?¹²⁰
- 121.** Basi wakaula wote wawili, na uchi wao ukawadhihirikia na wakaanza kujibandika

Na wao hawajui mipango yake na hikima zake.

111 Nyuso zitadhalilika Siku hii, na zitamnyenyekea Mwenyezi Mungu Aliye Hai asiye kufa, Mwenye kusimamia kupanga mambo yote ya viumbe vyake. Na amepoteza uwokofu na thawabu Siku ya Akhera mwenye kuidhulumu nafsi yake duniani, na akamshirikisha Mola wake Mlezi.

112 Na mwenye kutenda mambo ya ut'iifu, naye akawa anayasadiki aliyo yaleta Muhammad, s.a.w. huyo hana khofu ya kuzidishiwa makosa yake au kupunguziwa mema yake.

113 Na mfano wa maelezo haya ya haki yaliyo kwisha tangulia katika Sura hii, ya kumtukuza Mwenyezi Mungu, na hadithi ya Musa na khabari za Kiyama, Mwenyezi Mungu ameyeremsha katika Kitabu hichi cha Qur'ani kwa lugha ya Kiarabu, na ameeleza mara kwa mara kwa njia za kuonya ili watu waweze kutanabahi waache maasi, na Qur'ani iwazindue upya kwa kuwapa mawaidha na mazingatio.

114 Basi ametukuka na dhana dhana, na amejitenga na kushabihiana na viumbe, huyo Mfalme ambaye anahitajiwa na watawala na wanao tawaliwa, Mwenye haki katika Uungu wake na Utukufu wake. Na wewe, ewe Muhammad, usiifanyie haraka Qur'ani kabla Malaika hajakusomea. Na sema: Ewe Mola wangu Mlezi, nizidishie ilimu kwa Qur'ani na maana zake.

115 Ewe Mtume! Sisi tulimuusia Adam tangu mwanzo, asende kinyume na amri yetu, akasahau ahadi yetu akenda kinyume. Na hatukumwona tangu mwanzo wake kuwa ana azma baraabara, na ukakamavu wa kutosha asiingiliwe na Shetani akamtia wasiwasi katika nafsi yake.

116 Ewe Mtume! Na kumbuka pale Mwenyezi Mungu alipo waamrisha Malaika wamtukuze Adam kwa njia aliyo itaka Yeye *Subhanahu*, na wakafuata. Lakini Iblisi, naye alikuwa pamoja nao, alikuwa jini, akenda kinyume akakataa, akatolewa akafukuzwa!

117 Mwenyezi Mungu akamsemeza Adam kwa kumwambia: Hakika huyu Shetani aliye kwenda kinyume na amri yetu ya kukuadhimisha wewe ni adui yako wewe na Hawa, mkeo. Basi tahadhari na uchochezi wake kukuingizeni katika maasi, isije kuwa ndio sababu ya kutoka kwenu kwenye Bustani hii, ukaja pata taabu, ewe Adam, katika maisha baada ya kutoka kwenye Bustani.

118 Sisi tunakudhaminia mahitaji ya maisha yako katika Bustani. Humo hutopata njaa wala hutakuwa uchi.

119 Na wala hutopata kiu, wala hutopata joto la jua, kama wanavyo pata wanao sumbuka nje ya Bustani.

120 Shetani akamfanyia hila akimong'oneza katika roho yake, kumraghibisha yeye na mkewe, waule ule mti walio katazwa, akiwaambia: Ewe Adam! Mimi nitakuonyesha mti huo, ataye kula basi ataishi milele, na atapata ufalme usio na mwisho.

majani ya Bustani. Na Adam akamuasi Mola wake Mlezi, na akapotea njia.¹²¹

122. Kisha Mola wake Mlezi akamteuwa, naye akamkubalia toba yake, naye akamwongoa.¹²²

123. Akasema: Ondokeni humu nyote, hali ya kuwa ni maadui nyinyi kwa nyinyi. Na ukikufikieni uwongofu kutoka kwangu basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika.¹²³

124. Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.¹²⁴

125. Aseme: Ewe Mola wangu Mlezi! Mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona?¹²⁵

126. (Mwenyezi Mungu) atasema: Ndivyo vivyo hivyo. Zilikufikia ishara zetu, nawe ukazisahau; na kadhaalika leo unasahauliwa.¹²⁶

127. Na hivi ndivyo tutakavyo mlipa kila apitaye kiasi, na asiye amini ishara za Mola wake Mlezi. Na hakika adhabu ya Akhera ni kali zaidi, na inadumu zaidi.¹²⁷

128. Je! Haikuwabainikia tu; vizazi vingapi tuliviangamiza kabla yao, nao wanatembea katika maskani zao? Hakika katika hayo zimo ishara kwa wenye akili.¹²⁸

129. Na lau kuwa si neno lililo kwisha tangulia kutoka kwa Mola wako Mlezi na muda ulio wekwa, bila ya shaka inge fika adhabu (hapa hapa).¹²⁹

121 Akamwonyesha mti ulio katazwa. Adam na mkewe wakakhadaika kwa kudanganywa na Iblisi, na wakasahau makatazo ya Mwenyezi Mungu, na wakaula. Utupu wao ukadhihiri, kuwa ni malipo ya tamaa yao, mpaka wakasahau wakaingia katika ukhalifu. Wakawa wakikata majani ya miti ya Bustani ile ili wajisitiri utupu wao. Ikawa Adam kamkhaalifu Mola wake Mlezi. Hayo yalikuwa kabla hajapewa Unabii. Akayakosa maisha ya milele aliyo kuwa anayatamani, na yakaharibika maisha yake.

122 Kisha Mwenyezi Mungu alimteuwa ampe Utume, na akaipokea toba yake, na akamwongoa atake udhuru na aombe msamaha.

123 Mwenyezi Mungu aliwaamrisha Adam na mkewe watoke kwenye Bustani, wateremke kwenye ardhi, naye *Subhanahu* akawaambia kwamba utakuwapo uadui baina ya vizazi vyao, na kwamba Yeye *Subhanahu* atawaongoa kwa uwongofu na uwongozi. Mwenye kufuata uwongofu wa Mwenyezi Mungu hatoingia katika maasi duniani, wala hatoteseka kwa adhabu.

124 Na mwenye kujiepusha na uwongofu wa Mwenyezi Mungu na ut'iifu wake, basi ataishi maisha yasiyo na starehe, hatokinai na chochote anacho pewa na Mwenyezi Mungu, wala hatokuwa radhi na hukumu ya Mwenyezi Mungu na kudra yake. Mpaka ikija Siku ya Kiyama atakuja kwenye mkutano wa hisabu atashikwa kwa madhambi yake, naye hana hoja ya kutoa, kama alivyo kuwa duniani ni kipofu hazioni ishara zote za Mwenyezi Mungu.

125 Na kwenye mkutano huo atamuuliza Mola wake Mlezi kwa fazaa: Ewe Mola wangu Mlezi! Vipi umenisahaulisha hoja, hata nisiweze kujitolea udhuru, na umenisimamisha kama kipofu, na hali mimi duniani nilikuwa naona kila kitu, nikishindana na kutetea?

126 (Naye atajibiwa:) Mambo kwako ndivyo kama yalivyo. Zimekujilia dalili zetu, na Mitume wetu duniani; yote hayo ukayasahau, na ukajitia upofu, na hukuamini. Na leo basi kadhaalika unaachwa umesahauliwa umo katika adhabu na fedheha.

127 Na mfano wa malipo haya mabaya tunamlipa duniani mwenye kutenda maasi, na akamkadhibisha Mwenyezi Mungu na ishara zake. Na hakika adhabu za Akhera zina uchungu mkali zaidi, na zinadumu zaidi kuliko za dunia.

128 Vipi wanajitia upofu na ishara za Mwenyezi Mungu, na wanajua kuwa tumezihiliki kaumu nyingi zilizo tangulia kwa sababu ya ukafiri wao, nao hawakuwaidhika kwao juu ya kuwa wao wanapita wanatembea kwenye majumba yao na maskani zao, na wanayaona magofu yao na athari ya adhabu zilizo wapata? Hakika mambo kama hayo peke yake ni mawaidha kwa watu wenye akili za kufahamu.

129 Na lau kuwa haikutangulia hukumu ya Mola wako Mlezi ya kuwaakhirishia adhabu mpaka siku ya miadi maalumu, nayo ni Siku ya Kiyama, basi adhabu lazima ingeli wapata hapa hapa duniani kama ilivyo kwisha wapata makafiri wa karne zilizo pita.

130. Yavumilie haya wayasemayo. Na umtakase Mola wako Mlezi kwa kumsifu kabla ya kuchomoza jua, na kabla halijachwa, na nyakati za usiku pia umtakase, na ncha za mchana ili upate ya kukuridhisha.¹³⁰

131. Wala usivikodolee macho tulivyo wastareheshea baadhi ya watu miongoni mwao, kwa ajili ya mapambo ya duniani, ili tuwajaribu. Na riziki ya Mola wako Mlezi ni bora na inadumu zaidi.¹³¹

132. Na waamrishe watu wako kusali, na uendelee mwenyewe kwa hayo. Sisi hatukuombi wewe riziki, bali Sisi ndio tunakuruzuku. Na mwisho mwema ni kwa mchamngu.¹³²

133. Na walisema: Kwa nini hakutuletea muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Je! Haikuwafikilia dalili wazi ya yaliyomo katika Vitabu vya kale?¹³³

134. Na lau kuwa tuliwaangamiza kwa adhabu kabla yake, wangelisema: Ewe Mola wetu Mlezi! Kwa nini usituletee Mtume tukazifuata ishara zako kabla hatujadhilika na kuhizika.¹³⁴

135. Sema: Kila mmoja anangoja. Basi ngojeni! Hivi karibuni mtajua nani mwenye njia sawa na nani aliye ongoka.¹³⁵

130 Ewe Mtume! Vumilia hayo wayasemayo ya kukukadhibisha na kuukejeli Utume wako, na mtakase Mola wako Mlezi na yote yasiyo mfalia kwa kumsifu, na kumuabudu Yeye pekee daima, na khasa kabla ya jua kuchomoza, na kabla halijachwa. Na mtakase, umuabudu katika saa za usiku, na katika ncha za mchana kwa kusali, ili yadumu mawasiliano yako na Mwenyezi Mungu, upate kutua kwa hayo uliyo nayo, na uridhike kwa uliyo kadiriwa.

131 Wala usivuke mipaka kwa kuangalia yale mambo ya starehe ya namna mbali mbali tuliyo waonjesha makafiri. Kwani starehe hizi ni uzuri na pambo la duniani tu analo wafanyia mtihani kwayo Mwenyezi Mungu waja wake. Na Mwenyezi Mungu anakuwekea wewe Akhera yaliyo bora zaidi na yenye kudumu zaidi kuliko starehe hizi.

132 Na waelekeze ahli zako washike Sala kwa nyakati zake. Kwani Sala ni kiungo chenye nguvu kabisa cha kuwaunganisha na Mwenyezi Mungu, na kudumu kuishika Sala kwa nyakati zake ndio ukamilifu. Sisi hatukulazimishi ujiruzuku nafsi yako, bali ni Sisi ndio kazi yetu kukuruzuku. Na hakika mwisho wa kusifiwa duniani na Akhera ni wa watu wema na wenye kumcha Mungu.

133 Na makafiri katika inadi yao wanasema: Kwa nini Muhammad hatuletei dalili inayo toka kwa Mola wake Mlezi inayo tulazimisha sisi kumuamini? Na vipi wao wanaipinga Qur'ani, nayo imewajia hali imekusanya yaliyomo katika Vitabu vilivyo tangulia katika khabari za watu walio pita, na maangamizo yao kwa sababu ya kuwakadhibisha Mitume? Na Muhammad si wa kwanza katika hayo.

134 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu ange wafanyia haraka kuwahiliki makafiri hawa, kabla ya kumtuma Muhammad kwao, wange toa udhuru Siku ya Kiyama kwa kusema: Ewe Mola wetu Mlezi! Kwa nini hukutuletea Mtume duniani mwenye ishara tumfuate, kabla hujatuteremshia adhabu na hizaya Akhera? Lakini sasa hawana udhuru wowote baada ya kutumiwa Mtume.

135 Ewe Mtume! Waambie hawa wenye inda: Hakika sisi sote tunangojea yatavyo kwenda mambo yetu na yenu. Na mtajua kwa hakika nani katika makundi mawili walio watu wa Dini ya Haki, na wenye kuongoka kwa uwongofu wa Mwenyezi Mungu.

Sura 21 - Al-Anbiyaa

Utangulizi

HIINI SURA iliyo teremka Makka baada ya Surat Ibrahim. Aya zake ni 112. Inabainisha kukaribia Kiyama na hali washirikina wameghafilika nacho. Nao walidai kuwa Mtume hatokuwa binaadamu, na pengine wakisema kuwa hii Qur'ani ni uchawi, na pengine kuwa ni mashairi, na pengine ni ndoto za ovyo ovyo. Na maonyo yapo mbele yao. Na Mitume wote hawakuwa ila ni wanaadamu tu kama Muhammad s.a.w., na walio watangulia kabla yao walisema uwongo kama walivyo sema uwongo Makureshi. Mwenyezi Mungu aliwajaalia ajali yao, kwani Yeye ni Mweza wa kuteketeza na kubakisha, na ni vyake Yeye vyote viliomo katika mbingu na ardhi. Na Malaika kila walipo wanamtakasa kwa kumsabihi Mwenyezi Mungu Mtukufu wala hawasiti. Na hakika kwenda sawa mbingu na ardhi ni dalili kuwa Muumba wake ni Mmoja, kwani lau kuwa wangeli shirikiana waumbaji mambo yangeli fisidika. Na Mitume wote wamekuja na amri ya kuabudiwa Mwenyezi Mungu peke yake. Wala hana mwana, wala asiseme yeyote kuwa yeye ni mungu pamoja na Mwenyezi Mungu. Wasemao hivyo malipo yao ni Jahannamu. Na *Subhanahu* kabainisha utukufu wa viumbe vyake, na ajabu za uumbaji wake wa mbingu na ardhi. Na akabainisha hali ya washirikina na makafiri. Naye *Subhanahu wa Taa'la* amenabihisha vipi Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyo wahifadhi watu, na akaashiria *Subhanahu* nini malipo ya makafiri Siku ya Kiyama. Na akataja hadithi ya Musa na Harun pamoja na Firauni, na hadithi ya Ibrahim pamoja na kaumu yake, na alivyo mneemesha kwa dhuriya wema. Naye *Subhanahu wa Taa'la* ametaja hadithi ya Luut' na kaumu yake, na walivyo angamizwa, na hadithi ya Nuhu a.s. na ukafiri wa kaumu yake, na walivyo teketezwa isipo kuwa walio amini. Kisha *Subhanahu wa Taa'la* akaashiria hadithi za Sulaiman, na Daud, na Ayub, na Ismail, na Idris, na Dhulkifli, na Dhunnuun, na Maryamu. Na akataja khabari za Juj na Maajuj. Naye *Subhanahu* amebainisha vitendo vyema na matunda yake, na malipo watayo lipwa wenye kumchamngu na wakatenda mema, na hali yao Siku ya Kiyama, na rehema ya Mwenyezi Mungu katika Ujumbe wa Muhammad, na maonyo ya Mwenyezi Mungu kwa washirikina. Na kwamba hakika amri yote ni yake Yeye anavyo hukumu, na Yeye ndiye Mbora wa mahakimu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. IMEWAKARIBIA watu hisabu yao, nao wamo katika mghafala wanapuuza.¹
2. Hayawafikili mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao Mlezi ila huyasikiliza na huku wanafanya mchezo.²

1 Umewakaribia washirikina wakati wao wa kuhisabiwa Siku ya Kiyama, nao hali wameghafilika na kitisho chake, wanapuuza kuiamini.

2 Haiwajii Qur'ani kutokana na Mola wao Mlezi pale inapoteremka kuwakumbusha ya kuwanufaisha, ila wao huisikiliza na hali wao wameshughulika na mengine yasiyo na faida nao, wakicheza kama wachezavyo watoto wadogo.

3. Zimeghafilika nyoyo zao. Na wale walio dhulumu hunong'onezana kwa siri: Ni nani ati huyu isipo kuwa ni binaadamu tu kama nyinyi! Mnauwendea uchawi hali nanyi mnaona?³
4. Alisema: Mola wangu Mlezi anayajua yasemwayo mbinguni na katika ardhi. Na Yeye ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.⁴
5. Lakini wao walisema: Hizo ni ndoto za ovyo ovyo, bali amezizua tu, bali huyo ni mtunga mashairi. Basi atuletee miujiza kama walivyo tumwa wale wa mwanzo.⁵
6. Hawakuamini kabla yao watu wa mji tulio uangamiza. Basi, je, wataamini hawa?⁶
7. Na kabla yako hatukuwatuma ila watu wanaume tulio wapa wahyi (ufunuo). Basi waulizeni wenye ilimu ikiwa nyinyi hamjui.⁷
8. Wala hatukuwafanya miili isiyo kula chakula, wala hawakuwa wenye kuishi milele.⁸
9. Kisha tukawatimizia miadi, na tukawaokoa wao na tulio wataka, na tukawateketeza walio pita mipaka.⁹
10. Na hakika tumekuteremshieni Kitabu ambacho ndani yake yamo makumbusho yenu. Je! Hamzingatii?¹⁰
11. Na mingapi katika miji iliyo kuwa ikidhulumu tumeiteketeza, na tukawasimamisha baada yao watu wengine.¹¹
12. Basi walipo ihisi adhabu yetu, mara wakaanza kukimbia.¹²
13. Msikimbie! Na rejeeni kwenye zile zile starehe zenu, na maskani zenu,

3 Nyoyo zao zimo katika pumbao, hazizingatii, wameshikilia kuficha njama zao za kumpinga Nabii na Qur'ani, wakiambizana wenyewe kwa wenyewe: Huyu Muhammad si chochote ila ni mtu tu kama nyinyi. Na Mtume hawi ila Malaika. Basi, je! Mnamsadiki Muhammad na mnahudhuria baraza za uchawi na hali nyinyi mnaona kuwa hakika huo ni uchawi?

4 Mtume, kwa kuwa Mwenyezi Mungu kamjuulisha waliyo kuwa wakiyasema kwa siri, aliwaambia: Mola wangu Mlezi anayajua yote yanayo semwa katika mbingu na katika ardhi, na Yeye ndiye anaye sikia kila linalo sikiwa; na anajua kila linalo tokea.

5 Bali wao wakasema: Hizi ni mchanganyiko wa ndoto alizo ziota (Muhammad); bali kazua tu na akamsingizia Mwenyezi Mungu kwa uwongo. Kisha wakaacha hayo na wakasema: Bali huyu ni mtunga mashairi anaziteka nafsi za wenye kumsikiliza. Kama kweli, basi na atuletee muujiza khasa wa kuonyesha ukweli wake, kama walivyo tumwa Manabii wa zamani wakitiwa nguvu kwa miujiza mbali mbali.

6 Hizo kaumu tulizo ziangamiza baada ya kukadhibisha hiyo miujiza hazikuamini. Basi, je! Watakuja amini hawa yatapo wajia hayo wayatakayo?

7 Ewe Nabii! Kabla yako wewe hatukuwatumia watu ila watu wa kibinaadamu vile vile, ambao tuliwafunulia Dini waifikishe kwa watu. Basi, enyi mnao kataa! Waulizeni wanazuoni wajua ilimu za Vitabu vilivyo teremka, ikiwa nyinyi hamyajui hayo.

8 Wala Sisi hatukuwajaalia Mitume kuwa na miili inayo khitalifiana na miili ya wanaadamu wengine, wakawa wanaishi bila ya chakula, na wakabaki siku zote, na wala hawakuwa wanaishi daima milele.

9 Kisha tukawatimizia na tukawahakikishia ahadi, na tukawaokoa wao na pamoja nao tukawaokoa tulio taka kuwaokoa miongoni mwa Waumini. Na makafiri walio vuka mipaka tuliwaangamiza kwa kukadhibisha kwao na kuukataa Ujumbe wa Manabii wao.

10 Sisi hakika tumekuteremshieni Kitabu. Ndani yake yamo mawaidha ya kuwakumbusheni ikiwa mtakisoma na mtayatenda yaliyomo ndani yake. Basi huwaje mkakipuza na mkakikataa? Je, inda na upumbavu umefika hadi ya kukufikisheni hali hii mlilo nayo, mkawa hamuelewi lipi lenye manufaa nanyi mkalikimbilia?

11 Na wengi katika watu wa miji tuliyo iteketeza kwa sababu ya ukafiri wao na kuwakadhibisha Manabii, na baada yao tukasimamisha kaumu nyengine zenye hali bora na mwisho mwema kuliko hao.

12 Na tulipo taka kuwateketeza, na wakahisi ukali wa adhabu yetu na uwezo wetu wa kuwateremshia hayo yatakayo wapata, wakafanya haraka kukimbia, kama wanyama hayawani, ati kutafuta kuokoka!

mpatekusailiwa!¹³

14. Wakasema: Ole wetu! Hakika sisi tulikuwa madhaalimu.¹⁴

15. Hakikuacha hicho kuwa kilio chao mpaka tukawafanya kama walio fyekwa, wamezimika.¹⁵

16. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yao kwa mchezo.¹⁶

17. Kama tungeli taka kufanya mchezo tunge jifanyia Sisi wenyewe, lau kwamba tungeli kuwa ni wafanyao mchezo.¹⁷

18. Bali tunaitupa kweli juu ya uwongo ikauvunja na mara ukatoweka. Na ole wenu kwa mnayo yazua.¹⁸

19. Na ni vyake Yeye tu Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na katika ardhi. Na walioko kwake hawafanyi kiburi wakaacha kumuabudu, wala hawachoki.¹⁹

20. Wanamtakasa usiku na mchana, wala hawanyong'onyei.²⁰

21. Au wamepata miungu katika ardhi inayo fufua?²¹

22. Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subahana 'Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu, Bwana wa A'rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua.²²

23. Yeye hahojiwi kwa ayatendayo, na wao ndio wanao hojiwa kwa wayatendayo.²³

24. Au wanawaabudu miungu mingine badala yake? Sema: Leteni ushahidi wenu!

13 Enyi wapinzani! Msikimbie! Hapana kitu chochote kitacho kulindeni na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Rudini kwenye zile zile neema na majumba mliyo kuwa nayo, huenda watumishi wenu na wenzenu watakutakeni msaada na rai kama ilivyo kuwa ada yenu. Wapi! Hamtoweza!

14 Kwa kuwa hao makafiri wamekwisha sikia wanavyo kejeliwa na wanavyo itwa kwenda teketezwa na wana yakini nako, basi watasema: Hakika kweli sisi tulikuwa ni wenye kudhulumu tulipo yaacha yanayo tunafiisha, na tusiziamini Ishara za Mola wetu Mlezi.

15 Maneno hayo hawaachi kuyakariri na kuyapigia makelele mpaka kwa adhabu yetu tukawafanya kama mimea iliyo fyekwa, na moto ulio zimika, hawana tena uhai.

16 Wala hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo baina yao kwa mpango huu wa hikima, na muundo huu wa namna peke yake, kwa mchezo. Bali tumefanya yote haya kwa hikima ya juu ambayo wanaifahamu wenye kuzingatia.

17 Lau kuwa tunataka kufanya mchezo na pumbao isingeli mkinika kuchukua ila yaliyo katika ufalme wetu, kwani hapana ufalme ila wetu - ingeli kuwa Sisi ni wa kufanya hayo. Wala nasi si wenye kufanya hayo, kwa kuwa si laiki ya haki yetu.

18 Lakini jambo linalo tuelekea Sisi kulifanya ni kuipambanisha kweli juu ya uwongo ipate kuuondoa. Na nyinyi makafiri mtahiliki kwa sababu ya kumzulia Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

19 Na ni vya Mwenyezi Mungu peke yake vyote viliomo mbinguni na katika ardhi, kwa kuviumba na kuvimiliki. Basi ni haki Yeye peke yake kuabudiwa. Na Malaika walio karibishwa kwake hawana kiburi cha kuwazuia kumuabudu na kumnyenyekea, wala hawaoni machofu na kunyong'onyea kwa ibada ya mchana na usiku.

20 Wanamtakasa aliye tukuka shani yake na kila lisio muelekea. Kumtakasa huku hakusiti, bali huo ni mtakaso wa daima, hawana shughuli nyengine ya kuwashughulisha.

21 Washirikina hawafanyi wafanyavyo walio karibishwa katika kumsafishia ibada Mwenyezi Mungu, bali wao wamewaabudu wengine, na wakafanya miungu duniani isiyu stahiki kuabudiwa. Na huwaje kwenda kuabudu kitu kisicho kwa Mwenyezi Mungu, ambacho hakiwezi kufufua?

22 Lau kuwa mbinguni na duniani kuna miungu isipo kuwa Mwenyezi Mungu wanao endesha mambo yao, basi ingeli haribika nidhamu iliyo simamishiwa hizo mbingu na ardhi kwa kuumbwa, na ikafikilia mwisho wa mpango na hikima. Basi na atakasike Mwenyezi Mungu, Mwenye Ufalme wote, na yote wanayo msingizia washirikina.

23 Yeye *Subhanahu* hahojiwi kwa anayo yatenda, kwani ni Yeye pekee mwenye utukufu na madaraka, Mwenye hikima na ujuzi. Hakosei katika kutenda chochote. Ni wao ndio watahisabiwa na kuhojiwa kwa wanayo yatenda, kwa kuwa wao hukosea kwa udhaifu wao na ujinga wao na kughilibiwa na matamano.

Haya ni ukumbusho wa hawa walio nami, na ukumbusho wa walio kabla yangu. Lakini wengi wao hawajui kweli, na kwa hivyo wanapuuza.²⁴

25. Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.²⁵

26. Na wanasema: *Arrahman*, Mwingi wa Rehema, ana mwana! *Subhanahu*, Ametakasika na hayo! Bali hao (wanao waita wana) ni watumwa walio tukuzwa.²⁶

27. Hawamtangulii kwa neno, nao wanafanya amri zake.²⁷

28. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala hawamwombe yeyote ila yule anaye mridhia Yeye, nao kwa ajili ya kumwogopa wananyenyekea.²⁸

29. Na yeyote kati yao atakaye sema: Mimi ni mungu, badala yake, basi huyo tutamlipa malipo yake Jahannamu. Hivyo ndivyo tuwalipavyo wenye kudhulumu.²⁹

30. Je! Hao walio kufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi tukazibabandua? Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini?³⁰

31. Na tukaweka katika ardhi milima iliyo thibiti ili isiwayumbishe, na tukaweka humo njia pana ili wapate kuongoka.³¹

32. Na tukaifanya mbingu kuwa dari iliyo hifadhiwa, lakini wanazipuuza Ishara zake.³²

24 Hawajui waajibu wa Mwenyezi Mungu uliyo juu yao, ndio maana wakawa na miungu mingine isipo kuwa Yeye wakaiabudu bila ya kuwa na ushahidi wowote wa kuingia akilini, wala uthibitisho wa kweli. Ewe Nabii! Waambie: Leteni uthibitisho wenu kama kweli Mwenyezi Mungu ana mshirika katika utawala hata akafaa kushirikishwa katika kuabudiwa. Hii Qur'ani iliyo kuja kuukumbusha umati wangu kwa linalo wajibikia, na hivi Vitabu vya Manabii wengine vilivyo kuja kukumbusha kaumu za kabla yangu, vyote hivyo vimesimama juu ya Tawhid, Upweke wa Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui yaliyo kuja ndani ya Vitabu hivyo, kwa sababu hawajishughulishi kuyazingatia yaliomo humo. Basi wao wamekuwa wenye kuipuuza Imani ya Mwenyezi Mungu.

25 Ewe Nabii! Sisi hatukumtuma Mtume yeyote kabla yako ila tulimpa wahyi (ufunuo) awafikishie watu wake kuwa hastahiki kuabudiwa isipo kuwa Mimi. Basi nisafieni ibada, iwe kwangu tu.

26 Na baadhi ya makafiri wa Kiarabu walisema: *Arrahman*, Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, ana mwana, kwa yale madai yao kuwa Malaika ni binti za Mwenyezi Mungu. Ametakasika na kuwa na mwana! Kwani hao Malaika ni waja wake walio tukuzwa tu kwa kuwakaribisha, na kwa wanavyo muabudu Yeye.

27 Hawamtangulii Mwenyezi Mungu kwa kauli yao wainenayo kabla ya Yeye kuwapa ruhusa. Na wao hawatendi lolote ila kwa amri yake tu, wala hawapindikii mipaka ya amri anayo waamrisha.

28 Mwenyezi Mungu anazijua hali zao zote na vitendo vyao vyote, walivyo vitanguliza na walivyo viakhirisha. Wala hawamwombe mtu kwake ila kwa aliye ridhia Mwenyezi Mungu. Na wao jinsi ya wingi wa khofu yao kumwogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kumtukuza Yeye, daima wana hadhari naye.

29 Na miongoni mwa Malaika atakaye sema: Mimi ni mungu wa kuabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu, huyo tutamlipa kwa kumtia Jahannamu. Mfano wa malipo hayo tunamlipa kila mwenye kupindukia mipaka ya haki, na wakajidhulumu nafsi zao kwa kudai Ungu na kuingia katika ushirikina.

30 Wenye kukufuru wamepofuka, na hawaoni kuwa mbingu na ardhi hapo mwanzo zilikuwa zimeshikamana. Kwa uwezo wetu tukazibambandua mbali mbali. Na tukajaalia kutokana na maji, ambayo hayo si kitu hai, kila chenye uhai kutokana na hayo hayo. Basi je! Baada ya yote haya wangi kupuuza tu, na hawaamini kuwa bila ya shaka yoyote hapana mungu isipo kuwa Sisi? (*Tazama Maelezo 21:30*)

31 Na katika dalili za uweza wetu ni kuwa tumeifanya milima imesimama imara kwenye ardhi ili isiyumbeyumbe nao watu, na tumeifanya humo njia pana, za kupitia kwa wasaa, ili waweze kuongoza njia humo kwa makusudio yao. (*Tazama Maelezo 21:31*)

32 Na tumeifanya mbingu kama dari iliyo nyanyuliwa, na tukailinda isianguke, au visianguke viliomo humo. Na juu ya hayo, wao hawazioni wala hawazingatii Ishara zetu zenye kuonyesha uweza wetu na hikima yetu na rehema yetu. (*Tazama Maelezo 21:32*)

- 33.** Na Yeye ndiye aliye umba usiku na mchana na jua na mwezi, vyote katika anga vinaoagelea.³³
- 34.** Nasi hatukumjaalia mwanaadamu yeyote kabla yako kuwa na maisha ya milele. Basi je! Ukifa wewe, wao wataishi milele?³⁴
- 35.** Kila nafsi itaonja mauti; na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na kwetu Sisi mtarejeshwa.³⁵
- 36.** Na wakikuona walio kufuru hawakufanyi wewe ila ni kitu cha maskhara tu, (wakisema): Je! Ndiye huyu anaye itaja miungu yenu? Na hali wao wanakataa kumkumbuka *Arrahman*, Mwingi wa Rehema!³⁶
- 37.** Mwanaadamu ameumbwa na haraka. Nitakuonyesheni Ishara zangu. Basi msinihimize.³⁷
- 38.** Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa nyinyi mnasema kweli?³⁸
- 39.** Lau wangeli jua wale walio kufuru wakati ambao hawatauzuia Moto kwenye nyuso zao wala migongo yao, na wala hawatanusuriwa!³⁹
- 40.** Bali utawafikia kwa ghafla, na utawashitua na wala hawataweza kuurudisha, wala hawatapewa muhula!⁴⁰
- 41.** Na Mitume walio kabla yako walikwisha dhihakiwa. Kwa hivyo wale walio wafanyia maskhara yaliwafika yale waliyo kuwa wakiyafanyia dhihaka.⁴¹
- 42.** Sema: Nani anaye kulindeni usiku na mchana na *Arrahmani* Mwingi wa Rehema? Bali wao wanapuuza kumkumbuka Mola wao Mlezi.⁴²

33 Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye umba usiku na mchana, na jua na mwezi. Vyote hivyo vinakwenda katika njia zake kama alivyo zijaalia Mwenyezi Mungu, na zinamtakasa bila ya kupotea. (*Tazama Maelezo 21:33*)

34 Ewe Nabii! Hatukumjaalia mwanaadamu yeyote kabla yako wewe aishi milele, hata ikawa hao makafiri wakawa wanakutania ufe wewe. Vipi wanakutania mauti wewe na hali na wao vile vile watakufa kama wewe? Ukifa wewe, je, ndio wao watabakia kushinda wanaadamu wote?

35 Kila nafsi haina budi kuonja mauti. Na Sisi tunakufanyi hapa duniani kama wenye kukupeni mtihani, kwa kukupeni yenye manufaa yenu na yenye madhara pia, ili abagulike mwenye kushukuru kwa kupewa kheri na kuvumilia balaa, na yule asiye na fadhila kwa neema aipatayo na anapatika akipata misiba. Nanyi mtarejeshwa kwetu, na hapo tutakuhisabieni vitendo vyenu.

36 Na wakikuona, ewe Nabii, wale walio mkataa Mwenyezi Mungu na ulio kuja nayo wewe, hawakufanyii wewe ila maskhara na kejeli. Huambiana wao kwa wao: Ndiye huyu anaye watia aibu miungu yenu? Na hali wao hawasadiki kumdhukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye aliye waeneza rehema yake!

37 Na ikiwa wao wanataka waletewe adhabu kwa upesi, basi ndio tabia ya binaadamu kutaka kila jambo kwa haraka. Basi enyi wenye haraka! Nitakuonesheni neema yangu duniani, na adhabu yangu Akhera. Msijishughulisha kuhimiza kitu ambacho hakina budi kuwa. (*Tazama Maelezo 21:37*)

38 Na makafiri wanao himiza adhabu na huku wanaona haiwi, wanasema: Lini yatakuwa hayo mnayo tuahidi, enyi waumini, kama kweli hayo myasemayo?

39 Lau kuwa hao walio mkufuru Mwenyezi Mungu wangeli ijua hali yao wakati watapo kuwa hawawezi kuuondoa Moto kwenye nyuso zao na migongo yao, na wala hawampati wa kuwasaidia kuuondoa, wasingeli sema wayasemayo.

40 Kiyama hakiwajii kwa kukitarajia kutokea kwake, bali kitawazukia kwa ghafla tu kiwababaishe, wasiweze kukirudisha, wala wao hawatapewa muhula wa kutubia na kutafuta udhuru kwa waliyo kwisha yatenda.

41 Na Mitume wa kabla yako yaliwapata vile vile ya kufanyiwa kejeli na makafiri katika kaumu zao. Ikawateremkia hao walio wakataa Mitume na kuwafanyia maskhara adhabu hiyo hiyo ambayo wao waliifanyia maskhara na kejeli.

42 Ewe Nabii! Waambie: Ni nani anaye kuhifadhini na nakama zake wakati wa usiku na mchana, na akakurehemuni na kukuneemesheni? Hapana awezae hayo. Lakini wao wanaipuuza Qur'ani ambayo

43. Au wao wanao miungu watao weza kuwakinga nasi? Hao hawawezi kujinusuru nafsi zao, wala hawatalindwa nasi!⁴³
44. Bali tuliwastarehesha hawa na baba zao mpaka umri ukawa mrefu kwao. Je, hawaoni ya kwamba Sisi tunaifikia ardhi tukiipunguza ncha zake? Basi je! Hao ni wenye kushinda?⁴⁴
45. Sema: Mimi nakuonyeni kwa Wahyi. Na viziwi hawasikii wito wanapo onywa.⁴⁵
46. Na wanapo guswa na mpulizo mmoja tu wa adhabu itokayo kwa Mola wako Mlezi, bila ya shaka wao husema: Ole wetu! Hakika tulikuwa wenye kudhulumu.⁴⁶
47. Nasi tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali tutaileta. Nasi tunatosha kuwa washika hisabu.⁴⁷
48. Na kwa yakini tuliwapa Musa na Haaruni kipambanuzi, na mwangaza, na makumbusho kwa wachamngu,⁴⁸
49. Ambao wanamkhofu Mola wao Mlezi faraghani, na wanaiogopa Saa ya Kiyama.⁴⁹
50. Na haya ni makumbusho yaliyo barikiwa, tuliyo yateremsha. Basi je! Mnyakataa?⁵⁰
51. Na hakika tulikwisha mpa Ibrahim uwongofu wake zamani, na tulikuwa tunamjua.⁵¹
52. Alipo mwambia baba yake na watu wake: Ni nini haya masanamu mnayo yashughulikia kuyaabudu?⁵²

ndiyo inawakumbusha ya kuwafaa na kuwalinda na adhabu.

43 Kwani wao wanao miungu wa kuwalinda na adhabu itokayo kwetu? Hasha! Hiyo miungu yao haiwezi kujilinda wenyewe, licha kumlinda mwengineewe. Wala hapana yeyote awezae kumlinda yeyote kati yao karibu yake au pamoja naye pindi tukitaka kumuadhibu na kumteketeza.

44 Sisi hatufanyi haraka kuwaadhibu hawa kwa ukafiri wao, lakini tunawapururia na kuwastarehesha katika uhai wa dunia, kama tulivyo wastarehesha baba zao kabla yao, mpaka umri ukawa mrefu kwao. Je! Wanajitia upofu hawaoni yanao wazunguka wakaona kuwa Sisi tunaiendea nchi na tukaipunguza ncha zake kwa ushindi wa Waumini? Ni wao ndio wenye kushinda au Waumini ambao Mwenyezi Mungu amewaahidi kuwasaidia na kuwaunga mkono? (Tazama Maelezo 21:44)

45 Ewe Nabii! Sema: Sikuhadharisheni kwa maneno yanayo tokana nami. Lakini nakuhadharisheni kwa Wahyi (Ufunuo) unao tokana na Mwenyezi Mungu Mtukufu ulio njija mimi. Na huo ni wa Haki na kweli. Lakini hao kwa sababu ya kupuuzwa kwao kurefu kuipuuza Sauti ya Haki, Mwenyezi Mungu ameyaziba masikio yao mpaka wakawa kama viziwi. Na kiziwi hasikii Wito anapo hadharishwa na adhabu.

46 Na kuwa na yakini kuwa nao wakisisibiwa hata na chembe ya adhabu ndogo wanayo ifanyia maskhara, hupiga kelele kwa khofu wakisema: Ole wetu! Hakika sisi tulikuwa tunajidhulumu nafsi zetu, na tukiwadhulumu wenginewe, tulipo yakataa tuliyo ambiwa.

47 Na Sisi tunaweka mizani ya kupimiwa kwa uadilifu Siku ya Kiyama. Basi hadhulumiwi mtu kwa kupunguziwa wema wake au kuongezewa maovu yake. Hata ikiwa ni kiasi ya uzani wa chembe ndogo hii tutaileta na tutaihisabu. Na yatasha kuwa ni Sisi ndio wa kuhisabu. Basi hapana atakaye dhulumiwa kitu. (Tazama Maelezo 21:47)

48 Na Musa na Haaruni tuliwapa Taurati ya kupambanua baina ya kweli na uwongo, na halali na haramu. Na juu ya hivyo hiyo ni nuru ya kuwaongoa watu wafuate njia ya kheri na uwongozi mwema, na ni kumbusho la kuwafaa wachamngu.

49 Ambao wanamkhofu Muumba wao Mwenye kumiliki mambo yao yote, juu ya kuwa wako mbali na watu, na wala hawamwoni mtu. Nao wamo katika khofu ya daima kuikhofu Siku ya Kiyama.

50 Na hii Qur'ani ni kumbusho, lenye kheri nyingi. Tumekuteremshieni kama tulivyo mteremshia Musa. Basi yawaje nyinyi muikatae, na hali nyinyi ndio mnao stahiki zaidi kuiamini kuliko watu wote.

51 Na hakika Sisi tulikwisha mpa Ibrahim uwongofu na fikra ya kutafuta Haki kwa usafi wa niya kabla ya Musa na Haaruni. Na Sisi ni Wenye kujua vyema hali yake na fadhila zake zilizo mfanya astahiki kuchukua Utume.

52 Ewe Nabii! Kumbuka pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na watu wake kuwaonya juu ya masanamu waliyo kuwa wakishughulikia kuyaabudu: Ni nini haya masanamu ambayo nyinyi mmeshika

53. Wakasema: Tumewakuta baba zetu wakiyaabudu.⁵³
54. Akasema: Bila ya shaka nyinyi na baba zenu mmekuwa katika upotofu ulio dhaahiri.⁵⁴
55. Wakasema: Je! Umetujia kwa maneno ya kweli au wewe ni katika wachezao tu?⁵⁵
56. Akasema: Bali Mola wenu Mlezi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi ambaye ndiye aliye ziumba. Na mimi ni katika wenye kuyashuhudia hayo.⁵⁶
57. Na Wallahi! Nitayafanyia vitimbi masanamu yenu haya baada ya mkisha geuka kwenda zenu.⁵⁷
58. Basi akayavunja vipande vipande, ila kubwa lao, ili wao walirudie.⁵⁸
59. Wakasema: Nani aliye ifanyia haya miungu yetu? Hakika huyu ni katika walio dhulumu.⁵⁹
60. Wakasema: Tumemsikia kijana mmoja akiwataja. Anaitwa Ibrahim.⁶⁰
61. Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu, wapate kumshuhudia!⁶¹
62. Wakasema: Je! Wewe umeifanyia haya miungu yetu, ewe Ibrahim?⁶²
63. Akasema: Bali amefanya hayo huyu mkubwa wao. Basi waulizeni ikiwa wanaweza kutamka.⁶³
64. Basi wakajirudi nafsi zao, wakasema: Hakika nyinyi mlikuwa madhaalimu!⁶⁴
65. Kisha wakarejea kwenye ule ule upotovu wao wakasema: Wewe unajua kwamba hawa hawesemi.⁶⁵
66. Akasema: Basi nyinyi mnawaabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu wasio kufaini kitu wala kukudhuruni?⁶⁶

kuyaabudu?

- 53 Wakasema: Tumewakuta baba zetu wakiyatukiza na wameshika kuyaabudu. Nasi tukawafuata.
- 54 Yeye akasema: Nyinyi na baba zenu kabla yenu, ni wazi kuwa nyote mko mbali na Haki.
- 55 Wakasema: Je! Umetujia kwa haya uyasemayo na hakika ya kweli unayo iamini, au kwa maneno haya wewe ni katika wanao fanya pumbao na mchezo tu bila ya kuwa na maana yoyote?
- 56 Akasema: Hapana maskhara katika niyasemayo. Bali Mola wenu Mlezi anaye stahiki peke yake kutukuzwa na kuogopwa na kuabudiwa ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi, na akazileta bila ya kuwapo mfano wake wa kuigiza. Basi ni haki yake Yeye tu peke yake kuabudiwa. Na mimi kwa haya niyasemayo ni katika wenye hakika ambao hunena wanayo yashuhudia na wanayajua.
- 57 Na akasema moyoni mwake: Naapa kwa Mwenyezi Mungu, nitayafanyia vitimbi haya masanamu yenu niyavunje pale mtapo ondoka, ili mpate kuona upotovu wenu.
- 58 Baada ya kwish ondoka wale watu, Ibrahim aliyaendeya masanamu akayavunja vipande vipande, isipokuwa sanamu kubwa. Hilo aliliacha ili wapate kulirejea waliulize yalio isibu miungu yao. Nalo halikujibu kitu. Kwahivyo upotovu wa ibada yao ikabainika.
- 59 Baada ya kwisha ona yaliyo wapata miungu yao wakasema: Nani aliye itendea haya miungu yetu? Hakika mtu huyu hapana shaka ni katika walio jidhulumu wenyewe kwa adhabu itayo mpata..
- 60 Wakasema baadhi yao: Tumemsikia kijana mmoja akiitaja kwa kuisubu; naye anaitwa Ibrahim.
- 61 Wakasema wakubwa wao: Nendeni mkamlete, ahukumiwe mbele ya macho ya watu, na washuhudie aliyo yatenda!
- 62 Baada ya kwisha mhudhurisha, wakasema: Ni wewe ulio itenda haya miungu yetu, ewe Ibrahim?
- 63 Kuwanabihisha upotovu wao, alisema kwa kuwakejeli: Hili kubwa lao ndilo lililo tenda hayo! Iulizeni hiyo miungu aliyo yatenda huyu, kama kweli inaweza kujibu suala lenu!
- 64 Wakazirejea nafsi zao wakiifikiria ile ibada yao kuabudu vitu visivyo mnufaisha yeyote wala haviwezi kujitetea wenyewe. Wakayaona makosa yao. Baadhi yao wakasema: Ibrahim si katika walio dhulumu, bali nyinyi ndio madhaalimu kwa kuabudu vitu visio stahiki kuabudiwa.
- 65 Kisha wakarejea tena, wakaacha uwongofu, wakarudia upotovu. Wakamwambia Ibrahim: Hakika wewe umekwisha jua kuwa haya masanamu tunayo yaabudu hayasemi kitu. Basi vipi unatutaka tuyaulize?
- 66 Ibrahim akasema: Ikiwa hali yao haya masanamu ni hii, hayawezi kitu, na nyinyi ndio makhusiano yenu

67. Aibu yenu nyinyi na hivyo mnavyo viabudu badala ya Mwenyezi Mungu! Basi nyinyi hamtii akilini?⁶⁷
68. Wakasema: Mchomeni moto, na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo!⁶⁸
69. Sisi tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim!⁶⁹
70. Wao walimkusudia maovu, lakini Sisi tukawafanya wao ndio walio khasiri.⁷⁰
71. Na tukamwokoia yeye na Luut'i tukawapeleka kwenye nchi tulio ibariki kwa ajili ya walimwengu wote.⁷¹
72. Naye tukampa Is-haq, na Yaaqub kuwa ni ziada. Na wote tukawajaalia wawe watu wema.⁷²
73. Na tukawafanya maimamu wakiongoa watu kwa amri yetu. Na tukawafunulia watende kheri, na washike Sala, na watoe Zaka; na walikuwa wanatuabudu Sisi tu.⁷³
74. Na Luut'i tukampa hukumu na ilimu na tukamwokoia na ule mji ulio kuwa ukifanya maovu. Hakika hao walikuwa watu wabaya, wachafu.⁷⁴
75. Na tukamuingiza katika rehema yetu. Hakika yeye ni miongoni mwa watenda mema.⁷⁵
76. Na Nuhu alipo ita zamani, nasi tukamuitikia, na tukamwokoia yeye na watu wake kutokana na shida kubwa.⁷⁶
77. Na tukamnusuru na watu walio zikanusha Ishara zetu. Hakika hao walikuwa watu wabaya. Basi tukawazamisha wote.⁷⁷
78. Na Daud na Suleiman walipo kata hukumu katika kadhiya ya konde walipo lisha

nao ni hivi, basi nyinyi mmekuwa mnaacha kumuabudu Mwenyezi Mungu, na badala yake mnaabudu vitu visivyo kupeni faida hata chembe mkiviabudu, wala havikudhuruni kwa lolote mkiviachilia mbali?

67 Aibu yenu! Nyinyi na miungu yenu mmelaanika! Mnaacha fikra zenu zipotee, na mnapuuzza kuzingatia? Bila ya shaka haya masanamu hayafai kuabudiwa!

68 Wakaambiana wenyewe kwa wenyewe: Mchomeni moto mpate kuinusuru miungu yenu kwa mateso haya, ikiwa nyinyi mnataka kufanya kitu cha kuinusuru miungu yenu.

69 Sisi tukaufanya moto ule uwe baridi na salama, hauna madhara yoyote, kwa Ibrahim.

70 Wao walitaka kumuangamiza, lakini Sisi tukamwokoia, na tukawafanya wao ndio watu walio khasiri mno.

71 Na tukamwokoia yeye na Luut'i na njama zilizo pangwa, wakaelekea kwenye nchi tuliyo ijaalia kheri nyingi kwa watu wote, na tukawapeleka huko Manabii wengi.

72 Na tukampa Ibrahim mtoto Is-haq, na kutokana na Is-haq tukampa Yaaqubu, zaidi kuliko aliyo taka. Na wote wawili, Is-haq na Yaaqubu tuliwajaalia kuwa ni watu wema.

73 Na tukawafanya ni Manabii wakiwaendea watu, wakiwaongoa kwenye kheri kwa mujibu wa tulivyo waamrisha. Na tukawaonyesha vitendo vyema, na kudumisha Sala kama inavyo faa, na kutoa Zaka. Na wakawa wanatunyenyekea na kutusafia ibada Sisi tu.

74 Luut'i tukampa kauli ya kukata na madhubuti katika hukumu na ilimu yenye manufaa. Na tukamwokoia kutokana na mji ambao watu wake wanafanya kitendo cha namna ya peke yake katika uovu. Hakika hao walikuwa watu walio shikilia kufanya maovu, walio toka kwenye ut'iifu wa Mwenyezi Mungu na tabia iliyo zowewa.

75 Tukampeleka njia ya watu wa rehema yetu. Hakika huyo alikuwa miongoni mwa watu wema alio wakusanya Mwenyezi Mungu katika rehema yake na akawakunjulia msaada wake.

76 Na hapa tumtaje Nuhu wa kabila ya Ibrahim na Luut'i, pale alipo muomba Mola wake Mlezi aisafisha nchi kwa kuwaondoa waovu. Tukamuitikiya ombi lake, tukamwokoia yeye na wale walio amini katika watu wake, kutokana na shakawa ya kimbunga kikubwa.

77 Tukamlinda kwa nusura yetu na vitimbi vya kaumu yake walio zikanusha Ishara zetu zenye kuthibitisha Utume wake. Hakika hao walikuwa watu wa shari. Basi tukawagharikisha wote!

- humo mbuzi wa watu usiku. Na Sisi tulikuwa wenye kushuhudia hukumu yao hiyo.⁷⁸
79. Tukamfahamisha Suleiman. Na kila mmoja wao tulimpa hukumu na ilimu. Na tuliifanya milima na ndege kuwa pamoja na Daud imnyenyekee na imtakase Mwenyezi Mungu. Na Sisi ndio tulio fanya hayo.⁷⁹
80. Na tukamfundisha kuunda mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika kupigana kwenu. Je! Mtakuwa wenye kushukuru?⁸⁰
81. Na tukamsahilishia Suleiman upepo wa kimbunga wendao kwa amri yake kwenye ardhi tuliyo ibarikia. Na Sisi ndio tunao jua kila kitu.⁸¹
82. Na pia mashet'ani wanao mpigia mbizi na kufanya kazi nyenginezo. Na Sisi tulikuwa walenzi wao.⁸²
83. Na Ayyubu, alipo mwita Mola wake Mlezi, akasema: Mimi yamenipata madhara. Na Wewe ndiye unaye rehemu kuliko wote wanao rehemu.⁸³
84. Basi tukamwitikia, na tukamwondolea madhara aliyo kuwa nayo, na tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao kuwa ni rehema inayo toka kwetu, na ukumbusho kwa wafanyao ibada.⁸⁴
85. Na Ismail, na Idris, na Dhulkifli - wote walikuwa miongoni mwa wanao subiri.⁸⁵
86. Na tukawaingiza katika rehema yetu. Hakika wao walikuwa katika watu wema.⁸⁶
87. Na Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhibika, na akadhani ya kwamba hatutakuwa na uwezo juu yake. Basi aliita katika giza: Hapana mungu isipo kuwa Wewe *Subhanaka* Uliye takasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.⁸⁷

78 Ewe Nabii! Wataje Daud na Suleiman walipo toa hukumu katika kesi ya konde, ilio ingiliwa na mbuzi wa watu mbali usiku na wakala mazao yake. Na Sisi tulikuwa tunajua hukumu iliyo khusiana na kesi hiyo. (*Tazama Maelezo* 21:78)

79 Basi tulimfahamisha Suleiman hiyo *fatwa*. Na wote wawili tuliwapa hikima na ilimu ya maisha na mambo yake. Na tulimfanyia Daud pamoja na milima it'ii na imtakase Mwenyezi Mungu kama alivyo kuwa anamtakasa yeye Daud na kila lisio kuwa linamwelekea Mwenyezi Mungu. Na kadhaalika tuliwafanya ndege hivyo hivyo wamsabihi Mwenyezi Mungu pamoja naye. Na tulifanya hayo kwa uweza wetu usio shindika.

80 Tukamfundisha Daud kufuma nguo za chuma, ili zikulindeni katika vita vyenu. Basi mshukuruni Mwenyezi Mungu kwa neema hii aliyo kuneemesheni.

81 Na tulimsahilishia Suleiman upepo unao vuma kwa nguvu umtumikie, nao huo ulikuwa unakwenda kwa kufuata amri yake mpaka kwenye nchi tuliyo izidisha kheri yake. Nasi ni wenye kuyajua yote hayo. Halitupotei kubwa wala dogo.

82 Na tukawafanya mashetani wamtumikie kwa kuzamia chini baharini kumletea lulu na marijani; na wakifanya kazi nyenginezo, kama kujenga ngome na majumba ya kifalme. Na Sisi tulikuwa tukiwaangalia katika kazi zao hizo, basi hapana hata mmoja wao aliye pata shida, wala hawakuvunja amri ya Suleiman.

83 Ewe Nabii! Mtaje Ayyubu, pale alipo mwita Mola wake Mlezi, na maradhi yalikwisha mdhoofisha, na akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika nimesibiwa na madhara na yananiuma! Na Wewe ni Mbora wa wanao rehemu.

84 Tukamwitikia kwa aliyo yaomba, tukamwondolea madhara, na tukampa watoto kwa kadri ya waliyo kwisha kufa. Na tukamwongezea mfano wa wale, kuwa ni rehema iliyo tokana na fadhila yetu, na pia ni kuwa ni kumbusho kwa wengine wanao tuabudu ili wapate nao kusubiri kama alivyo subiri yeye, na watumai kupata rehema ya Mwenyezi Mungu kama alivyo tumai yeye.

85 Ewe Nabii! Watajie watu wako khabari za Ismail, na Idris, na Dhulkifli. Wote hao ni miongoni wanao subiri wakahimili taklifa na shida.

86 Na tukawajaalia miongoni mwa watu wa kupata rehema yetu. Hakika hao ni katika waja wetu wema.

87 Ewe Nabii! Taja kisa cha Yunus, aliye mezwa na samaki. Pale alipoona dhiki kwa vile watu wake walipo puuza wito wake, naye akawahama akenda mbali nao na huku amewakasirikia. Akadhani ya kuwa

88. Basi tukamwitikia na tukamwokoia kutokana na dhiki. Na hivyo ndivyo tunavyo waokoa Waumini.⁸⁸
89. Na Zakariya alipo mwita Mola wake Mlezi: Mola wangu Mlezi! Usiniache peke yangu, na Wewe ndiye Mbora wa wanao rithi.⁸⁹
90. Basi tukamwitikia, na tukampa Yahya na tukamponyeshea mkewe. Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea.⁹⁰
91. Na mwanamke aliye linda uke wake, na tukampulizia katika roho yetu, na tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni Ishara kwa walimwengu.⁹¹
92. Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi.⁹²
93. Nao wakalikata jambo lao hili mapande mapande baina yao. Wote watarudi kwetu.⁹³
94. Na atendaye mema naye ni Muumini basi haitakataliwa juhudi yake. Na hakika Sisi tunamwandikia.⁹⁴
95. Na haiwi kwa wana-mji tulio uangamiza, ya kwamba hawatarejea,⁹⁵
96. Mpaka watapo funguliwa Juju na Maajuju wakawa wanateremka kutoka kila mlima.⁹⁶

Mwenyezi Mungu amemruhusu kuwahama, na kwamba haitopita hukumu juu yake. Samaki akammeza, na akaishi katika kiza cha bahari. Akamwita Mola wake Mlezi kwa kumnyenyekea, na kuungama aliyokuwa nayo, akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Hapana wa kuabudiwa kwa haki ila Wewe. Ninakutakasa na kila lisio kuelekea Wewe. Ninaungama kuwa hakika mimi nilikuwa miongoni mwa walio dhulumu nafsi zao kwa kutenda yasio kupendeza.

88 Tukamwitikia kwa aliyokuwa akiyaomba, na tukamvua na dhiki aliyokuwa nayo. Na mfano wa hivi ndivyo tunavyo waokoa Waumini wanao ungama makosa yao, na wakatuomba kwa usafi wa moyo.

89 Na kitaje kisa cha Zakariya alipo mwita Mola wake Mlezi baada ya kwisha ona uweza wake *Subhanahu* kwa alivyo mtia katika nafsi yake matarajio ya rehema yake. Alisema: Ewe Mola wangu Mlezi! Usiniache mpweke bila ya kuwa na mrithi, na Wewe ndiye Mbora wa wanao rithi. Kwani Wewe ndiye utakaye baki baada ya kumalizika viumbe vyote.

90 Tukamtimizia matumaini yake, na tukamwitikia dua yake, na tukamtunukia juu ya ukongwe mwanawe, Yahya, tukamfanya mkewe tasa aweze kuzaa. Hakika wasafi hao Manabii walikuwa wepesi wa kutenda kheri tunayo itaka waitende, na wanatuomba kwa kutumai rehema yetu, na kuikhofu adhabu yetu. Na walikuwa hawamtukuzi mtu wala hawamwogopi mtu isipo kuwa Sisi tu.

91 Pamoja na hawa simulia kisa cha Maryamu aliye ulinda uke wake, nasi tukamfikishia siri katika siri zetu. Tukamjaalia achukue mimba bila ya mume, na tukamjaalia mwanawe azaliwe bila ya baba. Akawa yeye na mwanawe dalili iliyo wazi ya uweza wetu kugeuza sababu na vinavyo sabibishwa. Na hakika Sisi ni waweza wa kila kitu.

92 Hakika mila hii, nayo ndiyo Uislamu, ndiyo mila iliyo sahihi inayo kupasini kuilinda, kwa kuwa ni mila moja iliyo shikamana wala haikukhitalifiana baina ya hukumu zake. Basi nanyi msifarikieni katika mila hii kwa makundi na vyama. Na Mimi ndiye Muumba wenu, na Mwenye kumiliki mambo yenu yote. Basi niabuduni Mimi tu, wala msinshirikishe na mwengine.

93 Na juu ya kuwepo uwongozi huu aghlabu ya watu wamegawanyika kwa mujibu wa matamano yao, wakafanya mambo yao ya Dini mapande mapande, wakawa makundi mbali mbali. Na kila kundi litaturejea Sisi tulihasabia vitendo vyake.

94 Basi mwenye kutenda vitendo vyake vyema, naye ni mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Dini yake aliyokuwa iridhia, hatopunguziwa kitu katika juhudi yake. Bali atalipwa malipo kaamili. Na Sisi ni wenye kuiandika hiyo juhudi yake. Basi hakitopotea kitu.

95 Na haitakuwa kwa watu wa mji tulio uteketeza kwa sababu ya dhulma yao kwamba hawatarejea kwetu Siku ya Kiyama, bali hapana budi kuwa watarejea na tutawahisabia vitendo vyao viovu.

96 Mpaka itapo funguliwa milango ya shari na ufisadi, wakaingia wana wa Juju na Maajuju wakikimbizana kutemka milimani na majiani kwa kufanya vitendo vya fujo na rabsha.

97. Na miadi ya haki ikakaribia. Hapo ndipo yatapo kodoka macho ya walio kufuru (na watasema:) Ole wetu! Bila ya shaka tulikuwa tumeghafilika na haya, bali tulikuwa wenye kudhulumu.⁹⁷
98. Hakika nyinyi na hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannamu; huko mtaingia tu.⁹⁸
99. Lau kuwa hawa ni miungu, wasingeli ingia. Na wote watadumu humo.⁹⁹
100. Lao wao humo ni kupiga mayowe, na wala hawatasikia (jengino).¹⁰⁰
101. Ama wale ambao wema wetu umewatangulia, hao watatenganishwa na hayo.¹⁰¹
102. Hawatausikia mvumo wake, na wao watadumu katika yale zinayo yatamani nafsi zao.¹⁰²
103. Hicho Kitisho Kikubwa hakito wahuzunisha. Na Malaika watawapokea (kwa kuwaambia): Hii ndiyo Siku yenu mliyo kuwa mkiahidiwa!¹⁰³
104. Siku tutakapo zikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za vitabu. Kama tulivyo anza umbo la mwanzo tutalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu yetu. Hakika Sisi ni watendao.¹⁰⁴
105. Na hakika tulikwisha andika katika Zaburi baada ya Kumbukumbu, ya kwamba nchi watairithi waja wangu walio wema.¹⁰⁵
106. Hakika katika haya yapo mawaidha kwa watu wafanyao ibada.¹⁰⁶
107. Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.¹⁰⁷
108. Sema: Hakika imefunuliwa kwangu ya kwamba hakika Mungu wenu ni Mungu

97 Na ikakaribia miadi iliyo haina budi kutimizwa, nayo ni Siku ya Kiyama, wakawa wale walio kufuru wanakutikana wakikodoa macho yao kwa wingi wa kitisho, wakipiga makelele kusema: Kitisho gani hichi cha kutuagamiza! Hakika sisi tulighafilika na Siku hii. Bali tulikuwa ni wenye kujidhulumu nafsi zetu kwa ukafiri na inda.

98 Wataambiwa makafiri hawa: Nyinyi na hiyo miungu mliyo kuwa mkiiabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Moto wa Jahannamu. Nyinyi mtaingia humo muadhibiwe!

99 Lau kama hawa mlio waabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni miungu inayo stahiki kuabudiwa, wasingeli ingia nanyi humo. Na nyote, wenye kuabudu na kuabudiwa, mtabaki Motoni, wala hamtatoka.

100 Humo watatoa pumzi zitokazo vifuani kwa sauti kama ya mwenye kukabwa, kwa dhiki watayo pata, na hawatasikia la kuwafurahisha.

101 Hakika wale tulio wakubalia kwa kufuata kwao Haki na vitendo vya kheri, na tukawaahidi malipo mema, hao watawekwa mbali kabisa na Jahannamu na adhabu yake.

102 Hawatasikia sauti ya Moto wake unavyo vuma. Nao huko watapata kila ambacho nafsi inatamani, daima milele.

103 Hawato huzunishwa na Kitisho Kikubwa kinacho wafazaisha makafiri. Na Malaika watawapokea kwa kuwapongeza kwa kusema: Hii ndiyo Siku yenu ya neema aliyo kuaahidi Mola wenu Mlezi!

104 Siku tutapo zikunja mbingu kama zinavyo kunjwa karatasi katika kitabu. Na tutawarejeza viumbe kwa ajili ya hisabu na malipo. Wala hatushindwi kuwarejeza, kwani tuliwaumba mara ya kwanza. Na kama tulivyo waanza tutawarejeza. Ahadi yetu kwa hayo ni ahadi ya kweli. Daima Sisi tunatenda tunayo yaahidi.

105 Na tulikwisha andika katika Zaburi - nacho ni Kitabu cha Daud baada ya Taurati - kwamba nchi watairithi waja wangu walio wema wapate kuitengeza, na kusahilisha njia za maisha bora humo. ("*Bali wenye upole watairithi nchi*"..Zaburi 37.11 "*Wenye haki watairithi nchi, nao watakaa humo milele*"..Zaburi 37.29)

106 Hakika katika haya tuliyo yataja, khabari za Manabii pamoja na kaumu zao, na khabari za Pepo na Moto, yanatosha kuwakumbusha na kuwafanya wazingatie watu walio tayari kumuabudu Mwenyezi Mungu pekee na hawasalitiki na mapambo ya dunia.

107 Na hatukukutuma, ewe Nabii, ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote

Mmoja tu. Je! Mmesilimu?¹⁰⁸

109. Na kama wakigeuka, basi sema: Nimekutangazieni sawa sawa, wala sijui yako karibu au mbali hayo mliyo ahidiwa.¹⁰⁹

110. Hakika Yeye anajua kauli ya dhaahiri na anajua myafichayo.¹¹⁰

111. Wala sijui pengine huu ni mtihani tu kwenu na starehe mpaka muda kidogo.¹¹¹

112. Sema: Mola wangu Mlezi! Hukumu kwa haki. Na Mola wetu Mlezi ni Mwingi wa Rehema, aombwaye msaada juu ya mnayo yazua.¹¹²

108 Ewe Nabii! Sema: Hakika kiini cha Wahyi aliyo nipa Mwenyezi Mungu ni kwamba hakika nyinyi hamna Mungu isipo kuwa Yeye. Na yote yaliyo bakia niliyo funuliwa yanafuata asili hii. Ikiwa mambo ni hivyo, basi inakuwajibikieni mjisalimishe na mnyenyekee kwa Mwenyezi Mungu peke yake.

109 Wakito ujali wito wako, basi waambie: Nimekufunzeni yote aliyo niamrisha Mola wangu Mlezi; na kwa hivyo tumekuwa sawa kwa kuyajua hayo. Wala mimi sijui hayo ya kufufuliwa na kuhisabiwa mliyo ahidiwa, yatakuwa karibu au mbali.

110 Hakika Mwenyezi Mungu anayajua yote yasemwayo, mnayo yadhihirisha na mnayo yaficha.

111 Na sijui pengine huko kupewa muhula na kuakhirishiwa adhabu nyinyi ndio Mwenyezi Mungu anakufanyieni mtihani tu, na kukustarehesheni kwa ladha za maisha mpaka alipo kadiria Mwenyezi Mungu kukuhisabieni kwa hikima yake.

112 Ewe Nabii! Sema: Ewe Mola Mlezi! Tuhukumu baina yangu na hawa nilio wafikishia Wahyi kwa uadilifu ili wasiwe sawa Waumini na makafiri. Na Mola wetu Mlezi Mwenye kuneemesha kwa neema kubwa, Mwenye kustahiki kuhimidiwa na kushukuriwa, ndiye wa kutakiwa msaada kuvunja uzushi mnao zua, enyi makafiri.

Sura 22 - Al-Hajj

Utangulizi

Sura hii ni ya Madina ila Aya 52, 53, 54, na 55. Aya zake ni sabiini na nane. Imeanzia kwa kuwaonya watu wamkhofu Mwenyezi Mungu, na kukumbusha vitisho vya Kiyama, na kuwajuilisha wanao bisha kwa upotovu na ujinga, na hayo yakafuatia kuletwa dalili za kufufuliwa, kwa kuleta sura ya mabadiliko katika kuumbwa binaadamu na kukua kwa mimea, na ikaeleza upinzani kumpinga Mwenyezi Mungu, na matokeo yake. Na ikataja khabari ya Hija na kutukuza ibada zake. Na baada ya hayo Mwenyezi Mungu akaruhusu kupigana vita vya kujitetea. Na akafuatilia hayo kumpoza Mtume s.a.w. kwa masaiibu yaliyo kuwa yanampata kwa watu wake, kwa kutaja dhiki na mateso yaliyo wapata Mitume wa kabla yake. Na Aya za Sura hii zikabainisha dalili za uweza wake Mwenyezi Mungu Mtukufu na upweke wake, na mipaka ya kazi ya Mitume. Na kwamba hili ni onyo lisilo kimbilika. Na katika mwisho wa Sura wakasema hao wanao ambiwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu kwa kuzizuga akili za washirikina, kwamba hawawezi hata kuumba kiumbe kinyonge kabisa, naye ni nzi. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Na Sura ikahimiza Sala, na Zaka, na Ibada, na Jihadi, bila ya kukusudia maovu. Kwani hii ni Dini ya baba yenu Ibrahim aliye mzaa Ismail, ambaye kutokana naye ndio wakazalika ukoo wa A'dnan. Na matokeo ya mambo yenu ni kuwa Mtume wenu akushuhudieni kwa kukufikishieni Ujumbe, na nyinyi mtoe ushahidi juu ya watu walio kwisha tangulia kwamba Mitume wao waliwafikishia Ujumbe kama ilivyo kujieni katika Qur'ani. Na Sura ikakhitimisha kwa kutaka kushikamana na Mwenyezi Mungu. Kwani Yeye ndiye bora ya Mlinzi, na bora ya Mwenye kunusuru.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi. Hakika tetemeko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu.¹
2. Siku mtapo iona, kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshaye, na kila mwenye mimba ataharibu mimba yake. Na utaona watu wamelewa, na kumbe hawakulewa. Lakini adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali.²
3. Na miongoni mwa watu wapo wanao bishana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ilimu, na wanamfuata kila shet'ani aliye asi.³

1 Enyi watu! Tahadharini na adhabu ya Mola wenu Mlezi, na wekeni katika nyoyo zenu makumbusho ya Siku ya Kiyama. Kwani mtingishiko utao tokea hapo ni mkubwa, wenye kuhangaisha na kutikisa viumbe. 2 Siku mtapo kiona Kiyama mtaona kitisho chake kinafikilia ukubwa wake hata kama yupo mwanamke anaye nyonyesha na ziwa lake limo katika mdomo wa mwanawe, basi hapana shaka atamsahau na amwachilie mbali. Na kama yupo mwanamke ana mimba basi ataiharibu mimba kabla ya kufika wakati wake wa kuzaa kwa ajili ya fazaa na kitisho. Na ewe mwenye kuangalia! Ukiona hali ya watu Siku hiyo namna wanavyo onekana hawanazo, na wanapo kwenda wanayumba, utadhani wamelewa, na ilhali hawakulewa. Lakini kitisho walicho kishuhudia, na khofu ya adhabu kuu ya Mwenyezi Mungu ndiyo iliyo waondoshea utulivu wao.

3 Na juu ya onyo hili kali na la kweli bado wapo baadhi ya watu inadi yao au kufuata kwao kijinga

4. Ameandikiwa kwamba anaye mfanya kuwa rafiki, basi huyo hakika atampoteza na atamwongoza kwenye adhabu ya Moto mkali.⁴
5. Enyi watu! Ikiwa nyinyi mna shaka ya kufufuliwa basi kwa hakika Sisi tulikuumbeni kutokana na udongo, kisha kutokana na manii, kisha kutokana na kipande cha damu ilio gandana, kisha kutokana na kipande cha nyama chenye umbo na kisicho kuwa na umbo, ili tukubainishieni. Nasi tunakiweka katika matumbo ya uzazi tunacho kitaka mpaka muda ulio wekwa. Kisha tunakutoeni kwa hali ya mtoto mchanga, kisha mfikie kutimia akili. Na wapo katika nyinyi wanao kufa, na wapo katika nyinyi wanao rudishwa kwenye umri wa unyonge kabisa, hata mtu awe hajui kitu baada ya kuwa anakijua. Na unaiona ardhi imetulia kimya, lakini tunapo yateremsha maji juu yake husisimka na kututumka, na kumea kila namna ya mimea mizuri.⁵
6. Hayo ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu ndiye Haki, na kwamba hakika Yeye ndiye mwenye kuhuisha wafu, na kwamba hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.⁶
7. Na kwamba hakika Saa itakuja hapana shaka kwa hilo, na kwamba hakika Mwenyezi Mungu atawafufua walio makaburini.⁷
8. Na katika watu wapo wanao bishana juu ya Mwenyezi Mungu bila ya ilimu, wala uwongofu, wala Kitabu chenye nuru.⁸
9. Anaye geuza shingo yake ili kupoteza watu waache Njia ya Mwenyezi Mungu.

huwapelekea katika mambo ya kubishana juu ya Mwenyezi Mungu na sifa zake, wakamsingizia kuwa ati ana washirika, au wakaukataa uweza wake wa kufufua na kuwalipa watu kwa vitendo vyao. Na kwa huo ubishi wao na kukataa kwao hawategemei ilimu sahihi, au hoja ya kweli; lakini wao hufuata tu nyayo za kila shetani aliye muasi Mola wake Mlezi, aliye baidika na uwongofu.

4 Mwenyezi Mungu amehukumu kuwa anaye mfuata Shetani na akamfanya kuwa ni rafiki yake na mlinzi wake, na mwongozi wake, basi humpotoa na njia ya Haki, na akamuelekeza kwenye upotovu unao pelekea kwenye Moto unao waka na kuripuka.

5 Enyi watu! Ikiwa nyinyi mna shaka ya kukufufueni baada ya kufa, basi katika kuumbwa kwenu ipo dalili ya kuweza kwetu kufufua. Tulikuumbeni asili yenu kutokana na udongo, kisha tukaifanya tone ya manii, kisha baada ya muda tukaigeuza ikawa kipande cha damu iliyo gandana. Kisha tukaifanya kipande cha nyama yenye sura ya kibinaadamu, au isiyo kuwa na sura, ili tukubainishieni uweza wetu wa kuanza uumbaji na kuendeleza kukuza kwa viwango na madaraja, na kugeuza kutoka hali hii na kuingia nyengine. Na katika vilimo katika matumbo ya mzazi vipo tunavyo viharibu tuitakavyo na tunaviweka imara na madhubuti tuitakavyo, mpaka utimie muda wa kuzaliwa. Kisha tunakutoeni kwenye matumbo ya mama zenu muwe watoto wachanga. Kisha tunakuleeni mpaka mkamilike akili na nguvu. Na baada ya hayo wapo katika nyinyi ambao Mwenyezi Mungu huwafisha, na wapo ambao umri wao hurefushwa mpaka wakafikia ukongwe wa kupiswa, ujuzi wao na kufahamu kwao mambo kukasita. Na aliye kuumbeni kwa sura hii tangu mwanzo hashindwi kukurudisheni tena. Na jambo jengine la kukuonyesha kudra ya Mwenyezi Mungu kufufua ni kuwa wewe unaiona ardhi kavu yabisi; tukiiteremshia maji uhai unaitambalia, na hiyo ardhi hugutuka, na huzidi na hututumka kwa maji na hewa iliyo ingia ndani yake, na hapo tena hutokeza namna mbali mbali za mimea inayo furahisha kuiona, na uzuri wake ukazagaa, na mwenye kuiona roho yake ikakunjuka. (*Tazama Maelezo 22:5*)

6 Hayo yaliyo tangulia ya kuumbwa binaadamu, na mimea ya kupanda, ni ushahidi ya kwamba kwa hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mungu wa Haki. Na kwamba hakika Yeye ndiye anaye huisha maiti wakati wa kufufuliwa kama vile alivyo anza kuwaumba. Na kwamba hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu, na kwamba hakika Kiyama kinakuja tu bila ya shaka kuhakikisha ahadi yake. Na kwamba hakika Mwenyezi Mungu atawahuisha waliomo makaburini kwa kuwafufua kwa ajili ya hisabu na malipo.

7 Tazama tanbihi ya 6.

8 Na juu ya yaliyo tangulia bado wapo baadhi ya watu wanao jadili juu ya uweza wa Mwenyezi Mungu, na wanakanya kufufuka bila ya msingi wowote wa ki-ilimu, wala uwongozi wa kweli, au Kitabu kilicho toka kwa Mwenyezi Mungu cha kumwonyesha. Basi ubishi wake ni wa pumbao na inda tu.

Duniani atapata hizaya, na Siku ya Kiyama tutamwonjesha adhabu ya kuungua.⁹

10. (Ataambiwa): Hayo ni kwa sababu ya iliyo tanguliza mikono yako. Na hakika Mwenyezi Mungu si dhaalimu kwa waja.¹⁰

11. Na katika watu wapo wanao muabudu Mwenyezi Mungu kwa ukingoni. Ikimfikia kheri hutulia kwayo, na ukimfikia msukosuko hugeza uso wake. Amekhasiri dunia na Akhera; hiyo ndiyo khasara iliyo wazi.¹¹

12. Badala ya Mwenyezi Mungu, yeye huomba kisicho mdhuru wala kumnufaisha. Huko ndiko kupotelea mbali!¹²

13. Humuomba yule ambaye bila ya shaka dhara yake ipo karibu zaidi kuliko nafuu yake. Kwa hakika huyo ni mlinzi muovu, na rafiki muovu.¹³

14. Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walio amini na wakatenda mema katika Bustani zipitazo mito kati yake. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda atakayo.¹⁴

15. Anaye dhani kwamba Mwenyezi Mungu hatamnusuru (Mtume) katika dunia na Akhera na afunge kamba kwenye dari kisha aikate. Atazame je hila yake itaondoa hayo yaliyo mkasirisha?¹⁵

16. Na namna hivi tumeiteremsha (Qur'ani) kuwa ni Aya zilizo wazi, na hakika Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye.¹⁶

17. Hakika walio amini, na ambao ni Mayahudi na Wasabai na Wakristo na Majusi na wale walio shiriki - hakika Mwenyezi Mungu atawapambanua baina yao Siku ya

9 Na pamoja na hayo hugeuka upande kwa kiburi na kukataa kuikubali Haki. Na watu wa namna hii itakuja wapata hizaya na udhalili duniani kwa ushindi wa Neno la Haki, na Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atawaadhibu kwa Moto wa kuunguza.

10 Na ataambiwa: Hayo unayo yapata ya hizaya na adhabu ni kwa sababu ya uzushi wako na kiburi chako; kwani hakika Mwenyezi Mungu ni Muadilifu, hadhulumu. Wala hawaweki sawa Muumini na kafiri, na mwema na muovu; bali kila mmoja wao atamlipa kwa mujibu wa vitendo vyake.

11 Na miongoni mwa watu wapo wa namna ya tatu, ambao Imani bado haijatulia katika nyoyo zao, bali itikadi yao inayumba yumba. Maslaha ya nafsi zao ndiyo yanatawala katika Imani yao. Wakipata kheri hufurahi na hutulizana. Na wakipata shida yoyote katika nafsi zao, au mali zao, au wana wao, hurejea ukafirini. Hao huwa wamekosa duniani raha ya utulivu kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu na nusura yake, kama Akhera walivyo kosa neema ambayo Mwenyezi Mungu amewaahidi Waumini walio thibiti na wakasubiri. Hiyo khasara ya mara mbili ndiyo khasara ya kweli kweli iliyo wazi

12 Mwenye kukhasiri hivi humuacha Mwenyezi Mungu na akayaabudu masanamu yasiyo weza kumdhuru pindi akito yaabudu, wala hayamfai kitu pindi akiyaabudu. Kitendo chake huyo ndio kupotelea mbali na haki na uwongofu.

13 Badala ya Mwenyezi Mungu anamwomba ambaye madhara yake kwa kuharibu akili na kutawala mawazo ovyo ni karibu zaidi kwa nafsi kuliko kuitakidi msaada wake. Muabudiwa huyo ni muovu mno wa kumtaraji msaada, na muovu mno kumfanya rafiki.

14 Hakika wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake kwa Imani yenye kuambatana na vitendo vyema, Mola wao Mlezi atawatia Siku ya Kiyama katika Bustani zipitwazo chini ya miti yake na mito. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendavyo kumuadhibu mharibifu na kumlipa mema mtenda mema.

15 Ikiwa miongoni mwa makafiri yupo anaye dhani kwamba Mwenyezi Mungu hatamsaidia Nabii wake, basi na anyooshe kamba mpaka kwenye dari ya nyumba yake. Kisha ajinyonge, na akadirie katika nafsi yake na atazame, je, kitendo chake hicho kitaondoa hayo yanayo muudhi ya kuwa Mwenyezi Mungu anamnusuru Mtume wake?

16 Mfano wa tulivyo bainisha hoja zetu zi wazi katika tuliyo kwisha wateremshia Mitume. Tumemteremshia Muhammad Qur'ani yote, nayo ni Aya zilizo wazi ili ziwe ni hoja juu ya watu. Na hakika Mwenyezi Mungu humuongoa amtakaye kuwaongoa ili isalimike tabia yake na abaidike mbali na inadi na yanayo sabibisha hayo.

Kiyama. Hakika Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kila kitu.¹⁷

18. Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.¹⁸

19. Hawa wagomvi wawili walio gombana kwa ajili ya Mola wao Mlezi. Basi walio kufuru watakatiwa nguo za moto, na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yanayo chemka.¹⁹

20. Kwa maji hayo vitayayushwa viliomo matumboni mwao, na ngozi zao pia.²⁰

21. Na kwa ajili yao yatakuwapo marungu ya chuma.²¹

22. Kila wakitaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo, na wataambiwa: Onjeni adhabu ya kuungua!²²

23. Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walio amini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake. Watapambwa humo kwa mapambo ya mikononi ya dhahabu na lulu. Na mavazi yao humo ni hariri.²³

24. Na wataongozwa kwenye maneno mazuri, na wataongozwa kwenye Njia ya Msifiwa.²⁴

25. Hakika wale walio kufuru na wakazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu na Msikiti Mtakatifu, ambao tumeufanya kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakao humo na

17 Hakika wanao muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake wote, na Mayahudi wanao nasibika na Musa, na waabuduo nyota na Malaika, na Wakristo wanao nasibika na Isa, na Majusi wanao abudu moto, na washirikina wanao abudu masanamu, hakika wote hawa Mwenyezi Mungu atakuja wapambanua mbali mbali Siku ya Kiyama kwa kumdhihirisha mwenye haki na aliye potea kati yao. Kwani Yeye anajua vyema vitendo vyote vya viumbe vyake. Na atawalipa kwa vitendo vyao.

18 Ewe mwenye akili! Hujui kwamba hakika Mwenyezi Mungu vinamnyenyekea na kumt'ii vyote viliomo mbinguni na katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi katika watu wanamuamini Mwenyezi Mungu na wanafuata maamrishi yake, na kwa hivyo wanastahiki Pepo? Na wapo wengi miongoni mwao wanao puuza na wala hawamuamini, wala hawayatendi maamrishi yake, na kwa hivyo wanastahiki adhabu na hizaya. Na anaye fukuzwa na Mwenyezi Mungu kutokana na rehema yake basi hawezi yeyote kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu. Kwani Yeye hutenda ayapendayo.

19 Haya ni makundi mawili walio zozana kwa mambo yaliyo mkhusu Mola wao Mlezi, na yanayo mstahiki na yasio mstahiki. Kikundi kimoja kikamuamini na kikundi kingine kikakataa. Basi wale walio kataa na kukufuru Mwenyezi Mungu amewaandalia Siku ya Kiyama moto utao wazunguka na kuwapamba kila upande, kama nguo inavyo upamba mwili. Na kuzidi kuwaadhibu, Malaika watawamiminia maji ya moto mno juu ya vichwa vyao!

20 Yatawapenya mpaka kwenye matumbo yao, viliomo ndani viyayuke kama zitavyo yayuka ngozi zao!

21 Na pia wataandaliwa marungu ya chuma.

22 Kila wakijaribu kutoka Motoni kwa wingi wa machungu na dhiki Malaika watawapiga nayo hayo marungu, na watarudishwa huko waliko kuwako. Na watawaambia: Onjeni adhabu ya Moto unao unguza kuwa ni malipo ya ukafiri wenu.

23 Ama walio amini na wakatenda vitendo vyema, hao bila ya shaka Mwenyezi Mungu atawaingiza kwenye Mabustani yanayo pita mito kati ya majumba yake na miti yake. Humo watastarehe kwa kila namna ya starehe, na Malaika watawapamba vikuku vya mikono vya dhahabu na watawapamba kwa lulu. Ama nguo zao za kawaida zitakuwa za hariri.

24 Na ziada ya starehe yao humo Peponi ni kuwa Mwenyezi Mungu atawajaalia wawe na kauli njema, na vitendo vizuri vya kusifika. Basi watakuwa wakimtakasa Mwenyezi Mungu na kumtukuza, na watakuwa wenyewe kwa wenyewe wakiamiliana kwa mapenzi na amani.

wageni. Na kila atakaye taka kufanya upotofu humo kwa dhulma, basi tutamwonjesha adhabu chungu.²⁵

26. Na pale tulipomweka Ibrahim pahala penye ile Nyumba tukamwambia: Usinishirikishe na chochote; na isafishe Nyumba yangu kwa ajili ya wanao izunguka kwa kut'ufu, na wanao kaa hapo kwa ibada, na wanao rukuu, na wanao sujudu.²⁶

27. Na watangazie watu Hija; watakuja kwa miguu na juu ya kila ngamia aliye konda, wakija kutoka katika kila njia ya mbali.²⁷

28. Ili washuhudie manufaa yao na walitaje jina la Mwenyezi Mungu katika siku maalumu juu ya nyama hoa alio waruzuku. Basi kuleni katika hao na mlisheni mwenye shida aliye fakiri.²⁸

29. Kisha wajisafishe taka zao, na waondoe nadhiri zao, na waizunguke Nyumba ya Kale.²⁹

30. Ndio hivyo iwe! Na anaye vitukuza vitakatifu vya Mwenyezi Mungu basi hayo ndiyo kheri yake mbele ya Mola wake Mlezi. Na mmehalalishiwa nyama hoa ila wale mlilo somewa. Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu, na jiepusheni na usemi wa uwongo.³⁰

31. Kwa kumtakasikia Imani Mwenyezi Mungu, bila ya kumshirikisha. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wakamnyakua au upepo ukamtupa pahala mbali.³¹

25 Hakika wale walio kufuru, yaani walio mkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na pamoja na hayo wakawa mtindo wao kuwazuia watu wasiingie katika Uislamu, na kuwafanyia pingamizi Waumini kuingia kwenye Msikiti Mtakatifu wa Makka - na ilhali Mwenyezi Mungu ameufanya huo ni pahala pa amani kwa watu wote, mkaazi na mpita njia - atawapa watu hao adhabu kali. Na hali kadhaalika kila atakaye kengeuka na Haki, na akatenda udhalimu wowote katika pahala patakatifu, Mwenyezi Mungu atamuadhibu adhabu ya kutia chungu.

26 Ewe Nabii! Watajia hawa washirikina wanao dai kuwa ati wanamfuata Ibrahim a.s. na wakaifanya Nyumba Takatifu kuwa ni pahala pa kuwekea masanamu yao; watajia kisa cha Ibrahim na Nyumba Takatifu tulipo mwongoza mpaka pahala pake, na tukamuamrisha aijenge, na tukamwambia: Usinishirikishe Mimi na kitu chochote katika ibada. Na isafishe Nyumba yangu na masanamu na uchafu, ili iwe ni pahala pa makusudi ya mwenye kuizunguka kwa kut'ufu, na mwenye kukaa hapo na akafanya ibada.

27 Ewe Nabii! Wajuvye watu kwamba hakika Mwenyezi Mungu amewalazimisha wawezao miongoni mwao wajie hii Nyumba. Basi waitikie wito wako, watakuja kwa miguu na kwa kupanda ngamia aliye konda kwa ajili ya safari ya kutoka mbali.

28 Ili wapate manufaa yao ya Kidini kwa kutekeleza Hija na manufaa ya kiduniani kwa kujuana na ndugu zao Waislamu na kushauriana nao katika mambo ya Dini yao na dunia yao. Nao watajia jina la Mwenyezi Mungu katika Siku ya Idi Kubwa na siku tatu zifwatazo, pale wanapo chinja walio jaaliwa, ikiwa ngamia, au ng'ombe au kondoo na mbuzi. Kuleni mpendacho katika hao, na muwalishe walio patwa na shida na ufakiri.

29 Tena baada ya hao yawapasa waondoe takataka na uchafu ulio wapata wakati ule wa Ih'ram (yaani kuharimia Hija), nao ni majasho na safari ndefu. Pia waondoe nadhiri walizo mwekea Mwenyezi Mungu, ikiwa wameweka nadhiri yoyote. Na waizunguke kwa kwenda kwa miguu ile Nyumba iliyo jengwa kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu duniani.

30 Na mwenye kuzishika amri za Mwenyezi Mungu na makatazo yake katika Hija yake kwa kuzitukuza katika nafsi yake, hayo yatakuwa ni kheri yake katika dunia yake na Akhera yake. Na Mwenyezi Mungu amekuhalalishieni kula nyama hoa, (mifugo) yaani ngamia, ng'ombe, kondoo na mbuzi, ila katika hali mnazo zijua kwa mlivyo kwisha somewa katika Qur'ani, kama vile nyamafu na nyenginezo. Basi epukaneni na kuabudu masanamu, kwani ibada hiyo ni uchafu wa kiakili na kiroho, na haimwelekei mwanaadamu kufanya hivyo. Na epukaneni na kusema uwongo, kumzulia Mwenyezi Mungu au mwanaadamu.

31 Na kuweni wenye kumsafia niya Mwenyezi Mungu, wenye pupa kutaka kuifuata Haki, bila ya kumfuata mshirika wowote na Mwenyezi Mungu katika ibada. Kwani mwenye kumshirikisha Mwenyezi

- 32.** Ndio hivyo! Na anayetukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo.³²
- 33.** Katika hao nyinyi mna manufaa mpaka muda maalumu. Kisha pahala pa kuchinjiwa kwake ni kwenye Nyumba ya Kale.³³
- 34.** Na kila umma tumewafanyia mahala pa kuchinjia mihanga ya ibada ili walitaje jina la Mwenyezi Mungu juu ya vile walivyo ruzukiwa katika wanyama wa mifugo. Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Jisalimishieni kwake tu, na wabashirie wanyenyekevu,³⁴
- 35.** Ambao, anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hutetemeka, na wanao vumilia kwa yanao wasibu, na wanao shika Sala, na wanatoa katika tulivyo waruzuku.³⁵
- 36.** Na ngamia wa sadaka tumekufanyieni kuwa ni kudhihirisha matukuzo kwa Mwenyezi Mungu; kwa hao mna kheri nyingi. Basi litajeni jina la Mwenyezi Mungu juu yao wanapo simama kwa safu. Na waangukapo ubavu kuleni katika hao na walisheni walio kinai na wanao lazimika kuomba. Ndio kama hivi tumewafanya hawa wanyama dhalili kwenu ili mpate kushukuru.³⁶
- 37.** Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia uchamngu wenu. Namna hivi tumewadhililisha kwenu ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa alivyo kuongoeni. Na wabashirie wafanyao mema.³⁷

Mungu ameanguka huyo kutoka kwenye ngome ya Imani, na amesalitiwa na upotovu, na ameitia nafsi yake katika hilaki ya kutisha kabisa. Ikawa hali yake kama hali ya mtu aliye poromoka kutoka mbinguni na midege ikamraru akakatika mapande mapande, asibakie hata alama. Au kama aliye peperushwa na upepo mkali, na mwili ukatawanyika mwahala mbali mbali.

32 Hakika mwenye kuitukuza Dini ya Mwenyezi Mungu na faridha ya Hija na a'mali zake na mihanga inayo pelekwa kwa ajili ya mafakiri wa Al-Haram, na wakachagua walio nona wazima, hawana ila, basi huyo ndio amemcha Mwenyezi Mungu. Kwani kutukuza kwake hayo ni matokeo ya unyenyekevu wa nyoyo zilizo amini, na alama katika alama za usafi wa niya.

33 Katika kutoa mihanga hii yapo manufaa ya kidunia. Mnawapanda na mnakunywa maziwa yake mpaka wakati wa kuwachinja. Kisha mnapata manufaa ya Kidini vile vile pale mnapo wachinja kwenye Nyumba Takatifu kwa kutafuta kujikaribisha kwa Mwenyezi Mungu.

34 Hizi faridha za Hija hazikukhusuni nyinyi peke yenu. Kwani tumewajaalia jamaa wote walio amini mambo ya kuwakaribisha kwa Mwenyezi Mungu, na wanataja jina lake, na wanamtukuza wakati wanapo chinja kwa kumshukuru kwa neema aliyo waneemesha, na kuwasahilisha wanyama wa mifugo, nao ni ngamia, ng'ombe, mbuzi na kondoo. Na Mwenyezi Mungu aliye kuwekeeni sharia nyinyi na wao ni Mungu Mmoja. Basi yasalimisheni mambo yenu yote kwake Yeye peke yake. Na vitendo vyenu visafisheni kwake, wala msimshirikishe na yeyote. Na ewe Nabii! Wape bishara ya Pepo na thawabu nyingi wale walio safisha niya zao kwa Mwenyezi Mungu na wakawa wanamnyenyekea Yeye miongoni mwa waja wake.

35 Wale ambao akitajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hupapatika kwa kumkhofu, na hunyenyekea kwa kutajwa kwake, na ambao wanasubiri kwa masaibu ya karaha na shida yanayo wapata kwa kujisalimisha mbele ya amri yake na hukumu yake, na wakashika Sala kwa ukamilifu wake, na wakatoa baadhi ya mali aliyo waruzuku Mwenyezi Mungu katika njia za kheri.

36 Nasi tumefanya uchinjaji ngamia na ng'ombe n.k. katika Hija kuwa ni katika matukuzo ya Dini yalio dhaahiri. Na nyinyi kwa hayo mnajileta karibu na watu. Nanyi katika hao mnapata kheri nyingi katika dunia kwa kuwapanda, na kunywa maziwa yake. Na Akhera mnapata malipo na thawabu kwa kuwachinja na kuwalisha mafakiri. Basi tajeni jina la Mwenyezi Mungu wakati mnapo wapanga kwa safu kwa ajili ya kuwachinja. Mkisha wachinja kuleni sehemu mkitaka, na walisheni mafakiri walio kinai hawaombi, na ambao wanalazimika kuomba kwa haja. Na kama tulivyo fanya kila kitu kiwe kit'ifu kwa tuyatakayo kwa ajili ya manufaa yenu, na tumedhalilisha hivyo vikut'iini nyinyi ili mpate kuishukuru neema yetu kubwa iliyo juu yenu

37 Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu haangalii sura zenu wala vitendo vyenu, lakini anaangalia nyoyo

- 38.** Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walio amini. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila khaini mwingi wa kukanya mema.³⁸
- 39.** Wameruhusiwa kupigana wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia -³⁹
- 40.** Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa nyumba za wat'awa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi. Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu.⁴⁰
- 41.** Wale ambao tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Sala, na wakatoa Zaka, na wakaamrisha mema, na wakakataza mabaya. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote.⁴¹
- 42.** Na wakikukanusha basi walikwisha kanusha kabla yao watu wa Nuhu, na kina A'ad na kina Thamud,⁴²
- 43.** Na watu wa Ibrahim na watu wa Lut'i⁴³

zenu. Wala hataki kwenu mambo ya kujionyesha tu kwa kuchinja na kumwaga damu. Lakini anataka kwenu moyo wenye kunyenyekea. Basi hapati radhi yake mwenye kugawa hizo nyama wala damu. Lakini linalo pata radhi yake ni uchamngu wenu na usafi wa niya zenu. Kuwadhhalilisha hao wanyama tulivyo wadhhalilisha ni kwa ajili ya kukunafiisheni, mpate kumtukua Mwenyezi Mungu kwa vile alivyo kuongoeni hata mkatimiza ibada za Hija. Na ewe Nabii! Wape khabari njema watu wema walio tengeneza a'mali zao na niya zao kuwa watapata malipo makuu.

38 Hakika Mwenyezi Mungu huwalinda Waumini na huwahami na huwanusuru kwa Imani yao. Kwani Yeye hawapendi wenye kukhuni dhamana zao, wenye kupita mipaka katika ukafiri wao kumkataa Mola wao Mlezi. Na Mwenyezi Mungu hamsaidii yule asiye mpenda.

39 Mwenyezi Mungu amewaruhusu Waumini wanao pigwa vita na washirikina wawarejezee uadui wao, kwa sababu ya dhulma iliyo wapata nao wakasubiri kwa muda mrefu. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuweza kuwanusuru vipenzi vyake Waumini. (*Tazama Maelezo 22:39*)

40 Hao ambao makafiri wamewadhulumu na wakawalazimisha waache mji wao wa Makka wauhame. Na wao hawakuwa na kosa lolote ila ni kuwa walimjua Mwenyezi Mungu na wakamuabudu Yeye pekee. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hakuwatumilia kwa ajili ya Haki wasaidizi wa kumnusuru Yeye na wakamtetea kupinga jeuri za madhaalimu, basi hapana shaka upotovu ungeli enea, na majeuiri wangu endelea katika jeuri zao, na sauti ya haki wangu inyamazisha. Wala wasingeli achiliwa Wakristo makanisa yao, wala mamonaki (wat'awa wa Kikristo) wasingeli baki na monastari zao (nyumba zao za ibada), wala Mayahudi wasingeli kuwa na masinagogi yao, wala Waislamu wasingeli kuwa na misikiti yao, ambamo mote humo hutajwa kwa wingi jina la Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu amechukua juu ya nafsi yake ahadi ya nguvu ya kwamba atamsaidia na kumnusuru kila anaye isaidia Dini yake, na atamtukua kila mwenye kilitukua Neno la Haki katika ulimwengu. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu haiendi kinyume. Kwani Yeye ni Mwenye nguvu wa kutimiza alitakalo, Mtukufu hashindwi na yeyote.

41 Hao Waumini tulio waahidi kuwanusuru ndio hao ambao tukiwapa madaraka katika nchi wanalinda makhusiano yao na Mwenyezi Mungu na pia na wanaadamu wenzao. Kwa hivyo hushika Sala kwa utimilifu wake, na huwapa Zaka wanao stahiki kupewa, na huamrisha kila lenye kheri, na hukataza kila lenye shari. Na mambo yote hurejea kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Basi Yeye humtukua amtakaye, na humdhhalilisha amtakaye.

42 Ewe Nabii! Ukiwa unapata makanusho, kuambiwa mwongo, na maudhi kutokana na watu wako, basi usisikitike. Zingatia taarikh kwa yaliyo wapata Mitume wa kabla yako, utaona kwamba wewe si Mtume wa kwanza aliye kanushwa na kuudhiwa na watu wake. Kwani kabla ya hawa walio kukanusha wewe, kaumu Nuhu walimkadhibisha Mtume wao Nuhu, na kaumu ya A'ad walimkadhibisha Mtume wao Huud, na kina Thamud walimkanusha Mtume wao Saleh.

43 Na kaumu ya Ibrahim walimkanusha Mtume wao Ibrahim, na kaumu Lut'i walimfanyia hayo hayo

44. Na watu wa Madiana. Na Musa pia alikanushwa. Nikawapa muda makafiri, kisha nikawatia mkononi. Basi ilikuwaje adhabu yangu!⁴⁴
45. Miji mingapi tuliangamiza iliyo kuwa ikidhulumu, ikawa imebaki magofu, na visima vilivyo achwa, na majumba yaliyo kuwa madhubuti?⁴⁵
46. Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.⁴⁶
47. Na wanakuhimiza ulete adhabu, lakini Mwenyezi Mungu hatakwenda kinyume na ahadi yake kabisa. Na hakika siku moja kwa Mola wako Mlezi ni kama miaka elfu mnavyo hisabu nyinyi.⁴⁷
48. Na miji mingapi niliipa muda na hali ilikuwa imedhulumu, na kisha nikaitia mkononi? Na kwangu Mimi ndio marudio yote.⁴⁸
49. Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni mwenyaji kwenu niliye dhaahiri.⁴⁹
50. Basi walio amini na wakatenda mema watapata maghfira na riziki za ukarimu.⁵⁰
51. Na wanao jitahidi kuzipinga Aya zetu hao ndio watu wa Motoni.⁵¹

Mtume wao Lut'i.

44 Na watu wa Madiana walimkanusha Mtume wao Shua'ib. Na Firauni na watu wake walimkanusha Mtume wa Mwenyezi Mungu Musa. Mitume hao wote yaliwapata yanayo kupata wewe. Na Mimi niliwapata muhula hao wakanushao ili wapate kutubia waongoke, na waitikie Wito wa Haki. Lakini wakazua na wakaendelea na kuwakadhibisha Mitume wao na kuwaudhi. Wakazidisha madhambi juu ya madhambi yao. Basi nikawaadhibu ukomo wa kuwaadhibu. Angalia taarikhii yao utaona kuwa adhabu yangu ilikuwa kali mno, pale nilipo ibadilisha neema ikawa nakama, na uzima ukawa ni maangamizo, na badala ya ujenzi ukawa uharibifu.

45 Basi tuliwateketeza watu wengi wa miji ambayo waliamirisha, kwa sababu ya udhalimu wao na kukanusha kwao Mitume wao. Zikawa paa za nyumba zao zimeangukia kuta zake, hazina wakaazi. Kama kwamba jana hazikuwapo. Visima vingapi vilivyo bomoka na maji yake yakapotea, na majumba mangapi madhubuti yaliyo jengwa kwa mawe na saruji na chokaa, yamekuwa magofu hayana wakaazi!

46 Hivyo wao wanasema wayasemayo na wanahimiza waletewe adhabu, nao hawatembei ulimwenguni wakaona kwa macho yao walivyo teketea hao madhaalimu wakanushao? Huenda hapo nyoyo zao zikagutuka kutokana na ghafla iliyo wapamba, na wakatia akilini yanao wapasa wakafuata hayo ya wito wa Haki unao waitia. Na masikio yao yakisikia vifo vya hao makafiri huenda wao wakazingatia. Lakini wapi! Ya mbali hayo kuwa watu hawa waweze kuzingatia kwa wanayo yaona au kuyasikia maadamu nyoyo zao zimekuwa kama mawe. Kwani kipofu wa kweli siye yule aliye pofuka macho, lakini ni yule aliye pofuka moyo na hatambui kitu.

47 Na makafiri wa Makka wameshikwa na udanganyifu, na hawana wanalo litambua juu ya kuwepo dalili zote hizi. Kwa hivyo ndio wanakuhimiza, wewe Nabii, uwalettee adhabu ulio waahidi. Wanasema hayo kwa upinzani na kejeli. Na hayo hapana shaka yoyote yatawapata, lakini kwa wakati alio uweka Mwenyezi Mungu, ama duniani au Akhera. Naye hendi kinyume na ahadi yake, hata ikipita miaka. Kwani siku moja kwake ni kama miaka elfu mnavo ikadiria na kuihisabu. (*Tazama Maelezo 22:47*)

48 Na wengi katika watu wa mijini walikuwa madhaalimu kama wao. Nami nikawapa muhula wala sikuwafanyia haraka kuwaadhibu. Na kisha nikawateremshia hiyo adhabu. Na ni kwangu Mimi tu ndio marejeo ya wote Siku ya Kiyama; na hapo nitawalipa kwa wanayo stahiki. Basi enyi makafiri! Msighurike kwa kuchelewa adhabu kukufikieni.

49 Ewe Nabii! Waambie hao wanao kanusha, wanao kuhimiza waletewe adhabu: Sio kazi yangu mimi kukulipeni kwa vitendo vyenu. Bali hakika mimi ni mwenye kukuhadharisheni kwa hadhari iliyo wazi kwamba kuna adhabu. Na Mwenyezi Mungu ndiye wa kukuhisabuni na kukulipeni.

50 Na wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakatenda vitendo vyema, watapata kutokana na Mwenyezi Mungu kusamehewa dhambi zao walizo ziingia, kama kadhaalika watavyo pata riziki ya ukarimu huko Peponi.

51 Na wale walio jikukusa nafsi zao katika kuipiga vita Qur'ani kushindana na Waumini na kuwapinga, wakitamani na kudai kwa uwongo, kwamba wao watapata wayatakayo - watu hao watabaki milele katika

- 52.** Na hatukumtuma kabla yako Mtume wala Nabii ila anapo soma, Shet'ani hutumbukiza katika masomo yake. Lakini Mwenyezi Mungu huyaondoa anayo yatia Shet'ani; kisha Mwenyezi Mungu huzithibitisha Aya zake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.⁵²
- 53.** Hayo ni ili alifanye lile analo litia Shet'ani liwe ni fitna kwa wale wenye maradhi ndani ya nyoyo zao, na wale ambao nyoyo zao ni ngumu. Na hakika madhaalimu wamo katika mfarakano wa mbali.⁵³
- 54.** Na ili walio pewa ilimu wajue kuwa hayo ni Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi na waamini, na zipate kutua nyoyo zao. Na hakika Mwenyezi Mungu ndiye anaye waongoa wenye kuamini kwenye Njia Iliyo Nyooka.⁵⁴
- 55.** Na walio kufuru hawatoacha kuwa katika wasiwasi kwa hilo mpaka Saa iwafikie ghafla, au iwafikie adhabu ya Siku Tasa.⁵⁵
- 56.** Ufalme wote siku hiyo utakuwa wa Mwenyezi Mungu. Atahukumu baina yao. Basi walio amini na wakatenda mema watakuwa katika Bustani zenye neema.⁵⁶
- 57.** Na walio kufuru na kuzikanusha Ishara zetu, basi hao watapata adhabu ya kufedhehesha.⁵⁷
- 58.** Na walio hama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kisha wakauwawa au wakafa, bila ya shaka Mwenyezi Mungu atawaruzuku riziki njema. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mbora wa wanao ruzuku.⁵⁸
- 59.** Bila ya shaka atawaingiza pahala watakapo paridhia. Na hakika Mwenyezi Mungu

adhabu ya Motoni.

52 Ewe Nabii! Usihuzunike kwa hizi hila za makafiri. Yalimpata kama haya kila Mtume katika Mitume wetu, na kila Nabii katika Manabii wetu. Nayu ni kuwa kila wakiwasomea kitu kwa kuwaita waifuata Haki Mashetani wa kibinaadamu walio asi wakiyapinga ili waubat'ilishe Wito, na wawatie shaka watu kwa yale wanayo somewa. Makusudio yao ni kujiingiza kati baina ya Nabii na matamania yake ya kutaka Wito wake uitikiwe. Lakini Mwenyezi Mungu huyaondoa wayatakayo. Na mwisho Haki ndiyo inayo shinda anapo isimamisha Mwenyezi Mungu sharia yake, na akamnusuru Mtume wake. Na Yeye ndiye Mwenye kuzijua hali za watu na vitimbi vyao, Mwenye hikima katika vitendo vyake. Anaweka kila kitu pahala pake.

53 Na hakika Mwenyezi Mungu amewawezesha waasi wanao kataa Haki waweze kutumbukiza shakashaka na vikwazo katika Njia ya Wito ili uwe ni mtihamu na majaribio kwa watu. Makafiri ambao nyoyo zao zimegeuka mawe, na wanaafiki ambao nyoyo zao zina maradhi, huzidi upotovu kwa kueneza shakashaka hizi na kuziunga mkono. Na si ajabu madhaalimu hawa kusimama msimamo huu, kwani wao wamezama katika upotovu na wamevuka mpaka katika inadi na mfarakano.

54 Na ili walio pewa ilimu ya sharia na Imani wazidi Imani na kujua kwamba wayasemayo Mitume na Manabii hakika ni kweli iliyo teremka kutokana na Mwenyezi Mungu. Na kwamba Mwenyezi Mungu hakika anawalinda Waumini kwa hima yake kutokana na matatizo yote yanayo wapitikia. Na huwaongoa kwenye maarifa ya Njia Iliyo Nyooka nao wakaifuata.

55 Na walio kufuru hawatengenei. Bali wanaendelea kuitilia shaka Qur'ani mpaka wafikiwe na mauti, iwafikie adhabu ya Siku isiyokuwa na kheri kwao wala rehema; nayu ni Siku ya Kiyama.

56 Siku ambayo madaraka ya nguvu, na uendeshaji mambo usio na ukomo wote, ni wa Mwenyezi Mungu pekee. Siku hiyo ndipo atapo hukumu baina ya waja wake. Walio amini na wakatenda mema watadumu katika Bustani zilizo jaa kila namna ya neema.

57 Na walio kufuru na wakazikanusha Aya za Qur'ani tulizo mteremshia Muhammad, hao watakata adhabu ya madhila na fedheha.

58 Na wenye kuacha nchi zao kwa ajili ya kutukuza shani ya Dini yao wakitafuta radhi za Mwenyezi Mungu, kisha wakauliwa katika uwanja wa Jihadi, au wakafa vitandani mwao, Mwenyezi Mungu atawalipa malipo mazuri kabisa. Na hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mbora wa kutoa thawabu za ukarimu.

ni Mjuzi na Mpole.⁵⁹

60. Ndio namna hivi. Na anaye lipiza mfano wa alivyo adhibiwa, kisha akadhulumiwa, basi hapana shaka Mwenyezi Mungu atamsaidia. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mwenye maghfira.⁶⁰

61. Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu huingiza usiku katika mchana, na huuingiza mchana katika usiku, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.⁶¹

62. Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Wa Kweli, na kwamba wale wanao waomba badala yake, ni baat'ili, na hakika Mwenyezi Mungu ndiye Aliye Juu na ndiye Mkubwa.⁶²

63. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu huteremsha maji kutoka mbinguni, na mara ardhi inakuwa chanikiwiti? Hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole na Mwenye kujua.⁶³

64. Ni vyake viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Mwenye kusifiwa.⁶⁴

65. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu amevihalilisha kwenu viliomo katika ardhi, na marikebu zipitazo baharini kwa amri yake, na amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa idhini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye huruma kwa watu, Mwenye kurehemu.⁶⁵

59 Na hakika atawatia katika Pepo kwenye vyeo watavyo ridhika navyo na vitawafurahisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuzijua vyema hali zao, basi atawalipa malipo bora, naye ni Mpole huyasamehe makosa yao madogo madogo ya kuteleza.

60 Huo ndio mwendo wetu katika kuwalipa watu. Hatuwadhulumu. Na Muumini mwenye kulipiza kisasi kwa aliye mfanyia uovu, na akalipiza kwa kadri ya alivyo tendewa bila ya kuzidisha, kisha yule mkosa akaja kumfanyia uadui tena baada yake, basi hakika Mwenyezi Mungu anatoa ahadi ya nguvu kuwa atamnusuru na kumsaidia yule aliye dhulumiwa. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kumsamehe mwenye kulipiza kama alivyo dhulumiwa. Hamtii makosani kwa hayo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, basi huyasitiri makosa ya kuteleza ya mja wake mt'iifu, wala hamfedhehi Siku ya Kiyama.

61 Msaada huo ni mwepesi kwa Mwenyezi Mungu, kwani Yeye ni Muweza wa kila kitu. Na katika Ishara za uwezo wake zilio wazi mbele yenu ni utawala wake juu ya ulimwengu wote. Huzungusha usiku na mchana, pengine huzidi huu au huzidi huu. Inakuwa baadhi ya kiza cha usiku pahala pa mwanga wa mchana. Na pengine huwa kinyume cha hivyo. Naye *Subhanahu* juu ya uwezo wake husikiliza kauli ya aliye dhulumiwa, na anaviona vitendo vya mwenye kudhulumu. Basi humtia adhabuni.

62 Huo ndio msaada wa wenye kudhulumiwa unao tokana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kutenda kwake katika ulimwengu kama atakavyo bila ya kiwango ni kama muonavyo matokeo yake; na kwa hakika Yeye ndiye Mungu wa Haki ambaye hapana mungu mwenginewe pamoja naye. Na kwamba masanamu wanayo yaabudu washirikina ni uwongo, hayana ukweli, na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye tukuka juu ya vyote isipo kuwa Yeye Mwenyewe kwa shani yake, na ni Mkuu wa madaraka.

63 Ewe mwenye akili! Huzingatii haya yalio kuzunguka uyaonayo kwa macho yenu kuonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu, ukamuabudu Yeye peke yake? Yeye ndiye anaye iteremsha mvua kutoka mawinguni, na ardhi ikageuka rangi ya kijani kibichi kwa mimea inayo chipuka, baada ya kuwa na ukame. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole mno kwa waja wake, na anajua vyema yanayo wanufaisha na kwa hivyo akawatengeneza kwa kudra yake.

64 Kila kiliomo mbinguni na katika ardhi ni chake Yeye, na kinamtumikia Yeye peke yake, na anakiendesha kama apendavyo. Na Yeye hawahitajii waja wake, bali wao ndio wanao mhitajia Yeye. Na Yeye ndiye anaye stahiki peke yake kuhimidiwa na kusifiwa na viumbe vyote.

65 Ewe mwenye akili! Huyaangalii yaonekanayo kwa macho ya uwezo wa Mwenyezi Mungu, ukaona anavyo wasahilishia watu wote kunafiika na ardhi na viliomo ndani yake? Na akawatengeneza bahari za kwendea ndani yake marikebu kwa mujibu apendavyo Yeye? Na akazishika sayari zote ziliomo angani kwa kudra yake hata zisikosee mpango wake, au zikaangukia kwenye ardhi, isipo kuwa akitaka kwa mapenzi yake. Hakika Mwenyezi Mungu Aliye takasika ni Mwingi wa huruma na rehema kwa waja wake. Kwa hivyo amewatengeneza kila njia za maisha mema. Huwaje basi baada ya haya yote

66. Na Yeye ndiye aliye kuhuisheni kisha akakufisheni, na kisha atakufufueni. Hakika mwanaadamu hana fadhila.⁶⁶
67. Kila umma tumewajaalia na ibada zao wanazo zishika. Basi wasizozane nawe katika jambo hili. Na waite watu kwendea kwa Mola wako Mlezi. Hakika wewe uko kwenye Uwongofu Ulio Nyooka.⁶⁷
68. Na wakikujadili basi sema: Mwenyezi Mungu anajua zaidi mnayo yatenda.⁶⁸
69. Mwenyezi Mungu atahukumu baina yenu Siku ya Kiyama katika hayo mnayo khitalifiana.⁶⁹
70. Je! Hujui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliomo mbinguni na katika ardhi? Hakika hayo yamo Kitabuni. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.⁷⁰
71. Na wanaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ambavyo hakuviteremshia ushahidi, na ambavyo hawana ujuzi navyo. Na madhaalimu hawatakuwa na wa kuwasaidia.⁷¹
72. Na wanapo somewa Aya zetu zilizo wazi utaona chuki katika nyuso za walio kufuru. Hukaribia kuwavamia wale wanao wasomea hizo Aya zetu. Sema: Je! Nikwambieni yaliyo mabaya zaidi kuliko haya? Ni Moto. Mwenyezi Mungu amewaahidi walio kufuru, na ni marudio mabaya hayo.⁷²
73. Enyi watu! Unapigwa mfano, basi usikilizeni. Hakika wale mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, hawatoumba hata nzi ijapo kuwa watajumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Amedhoofika kweli huyo mwenye

hamumsafii niya Yeye kwa kumshukuru na kumuabudu? (*Tazama Maelezo 22:65*)

66 Na Yeye ndiye aliye kupeni uhai. Kisha anakufisheni unapo malizika muda wenu. Kisha tena atakufufueni Siku ya Kiyama kwa ajili ya hisabu na malipo. Hakika mwanaadamu baada ya neema zote hizi na ushahidi wote huu ni mwingi wa kumkataa Mwenyezi Mungu na kuzikataa neema zake alizo mpa.

67 Tumewajaalia katika kila umma walio kwisha tangulia wawe na sharia zao makhsusi zinazo ambatana na zama zao, za kumuabudia Mwenyezi Mungu, mpaka zinapo kuja futwa na zijazo baadae. Na kwa hivyo tumewajaalia watu wako, ewe Nabii, wawe na Sharia ya kumuabudu Mwenyezi Mungu mpaka Siku ya Kiyama. Iliyoy kuwa hivi ndio amri yetu na mpango wetu, basi hao wanao jiabudia kwa dini zao zilizo pita, haiwafalii wao kutia mkazo katika kukupinga wewe. Kwani hakika sharia yako wewe imefuta sharia zao. Basi usijishughulisha na kujadiliana nao. Nawe endelea kuwaita watu wende kwa Mola wako Mlezi kwa mujibu wa unavyo pewa wahyi (ufunuo). Hakika wewe unafuata Uwongofu Ulio Nyooka wa Mola wako Mlezi.

68 Na wakishikilia kuendea kukujadili basi waachilie mbali, na waambie: Mwenyezi Mungu anajua zaidi vitendo vyenu, na malipo mnayo yastahiki.

69 Mwenyezi Mungu atahukumu baina yangu na nyinyi Siku ya Kiyama katika hayo mnayo khitalifiana nami. Atamlipa thawabu aliye ongoka na atamuadhibu aliye potoka.

70 Ewe mwenye akili! Jua kuwa ujuzi wa Mwenyezi Mungu umekusanya kila kiliomo mbinguni na duniani. Hapana kitendo cha hawa washindani kinacho fichika kwake. Vyote hivyo vimekwisha andikwa katika Ubao ulio hifadhiwa (*Lauhun Mahfuudh*). Kwani kujua kwake Mwenyezi Mungu na kuvithibiti kwake ni kazi nyepesi kabisa kwake.

71 Na washirikina huabudu badala ya Mwenyezi Mungu masanamu na watu ambao haikuteremka hoja yoyote ya kuwaabudu hao katika Kitabu cha mbinguni chochote. Wala wao hawana ushahidi wowote wa kuingia akilini. Lakini wanafanya yote hayo kufuata pumbao na mila tu. Wala hao washirikina walio zidhulumu nafsi zao na wakazidharaulisha akili zao hawato pata msaidizi wa kuwanusuru, na kuwakinga na adhabu ya Moto Siku ya Kiyama, kama wanavyo jidai.

72 Ewe Nabii! Hawa washirikina mtu akiwasomea Aya zetu zilizo wazi, na ambazo ndani yake mna ushahidi wa ukweli wa hayo unao waitia, na ubaya wa ibada zao, utaona katika nyuso zao ghadhabu na chuki inayo wajaa, hata inakaribia kuwapelekea kutaka kumuwa huyo anaye wasomea. Ewe Nabii! Waambie kwa kuwazindua na kuwaonya: Je! Mtanisikiliza nikwambieni yaliyo kuwa mabaya zaidi kuliko hiyo chuki inayo kuunguzeni roho? Ni Moto ambao Mwenyezi Mungu amewaahidi walio kufuru kama nyinyi Siku ya Kiyama. Na hapana mwisho mbaya na makaazi maovu kuliko hayo.

kutaka na mwenye kutakiwa.⁷³

74. Hawakumuadhimisha Mwenyezi Mungu anavyo stahiki kuadhimishwa. Hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mwenye kushinda.⁷⁴

75. Mwenyezi Mungu huteuwa Wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.⁷⁵

76. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Na kwa Mwenyezi Mungu yatarejeshwa mambo yote.⁷⁶

77. Enyi mlio amini! Rukuuni na msujudu, na muabuduni Mola wenu Mlezi, na tendeni mema, ili mfanikiwe.⁷⁷

78. Na fanyeni juhudi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama inavyo stahiki jihadi yake. Yeye amekuteueni. Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim. Yeye (Mwenyezi Mungu) alikuiteni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Qur'ani) pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu, na nyinyi muwe mashahidi kwa watu. Basi shikeni Sala na toeni Zaka na shikamaneni na Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mlinzi wenu, Mlinzi bora kabisa, na Msaidizi bora kabisa.⁷⁸

73 Enyi watu! Sisi tunakufahamisheni ukweli wa ajabu, basi hebu usikilizeni na muuzingatie. Haya masanamu hayataweza kabisa kuumba chochote hata kikiwa kitu duni kabisa kama nzi; hata ikiwa yote yakisaidiana katika kuumba huko. Bali huyu makhluku duni kabisa akiwanyang'anya chochote katika hizo sadaka wanazo pewa masanamu hawawezi kumzuia au kumfukuza. Unyonge gani basi huwa wala kushindwa na nzi kutoweza kurejesha alichopo pokonya. Na nzi ni kitu dhaifu mno! Wote wawili ni wanyonge. Bali hayo masanamu ambayo kama mnavyo ona ni dhaifu zaidi, basi huwaje mwanaadamu mwenye akili akenda kuyaabudu na kutaka yamnafiishe.

74 Hawa washirikina hawamjui Mwenyezi Mungu kama anavyo faa kujuulikana, wala hawamtukuzi kama anavyo stahiki kutukuzwa, walipo kwenda kumshirikisha katika ibada na vitu visio kuwa na maana kabisa. Na hali kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Muweza wa kila kitu, Asiye shindika na yeyote.

75 Mapenzi ya Mwenyezi Mungu na hikima yake yamempelekea kuteuwa Wajumbe kutokana na Malaika, na kutokana na wanaadamu, ili wafikishe sharia yake kwa viumbe vyake. Basi huwaje mkampinga aliye mchagua Mwenyewe kuwa ni Mjumbe wake kwenu? Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyasikia wayanenayo waja wake, Mwenye kuviona vitendo wavitendavyo. Naye atawalipa kwavyo.

76 Na Yeye *Subhanahu* anajua hali zao zilizo dhaahiri na za ndani. Hapana kinacho fichika kwake. Na kwake Yeye pekee ndiyo yanarejea mambo yote.

77 Enyi mlio amini! Msishughulikie upotovu wa makafiri. Nyinyi endeleeni na kutimiza Sala zenu kwa ukamilifu kwa kurukuu na kusujudu. Na muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni na akakuruzukuni. Wala msimshirikishe naye na yeyote. Na tendeni kila lenye kheri na manufaa, ili mpate kuwa watu wema, walio bahatika katika Akhera yenu na dunia yenu.

78 Na wanieni katika Jihadi ya kunyanyua Neno la Mwenyezi Mungu na kutafuta radhi zake mpaka mwashinde maadui zenu na myashinde matamano yenu. Kwani Yeye *Subhanahu* amekukaribisheni kwake, na amekuteueni muinusu Dini yake, na amekujalieni muwe Umma wa katikati. Wala hakukulizimisheni katika aliyo kuwekeeni Sharia lolote lenye mashaka juu yenu msilo weza kulichukua. Na amekufanyieni mepesi katika yanayo kuleteeni mashaka, na katika msiyo yaweza amekufanyieni ruhusa namna mbali mbali. Basi ishikeni Dini hii, kwani hii ndiyo Dini ya baba yenu Ibrahim katika misingi yake. Na Yeye *Subhanahu* ndiye aliye kuiteni Waislamu, (yaani Wanyenyeketu) katika Vitabu vya mbinguni vilivyo tangulia, na pia katika hii Qur'ani kwa ut'iifu wenu kwa yale aliyo kutungieni sharia. Basi kueni kama alivyo kuiteni Mwenyezi Mungu ili muwe mwisho wenu mnamshuhudia Mtume kama amekufikishieni ujumbe nanyi mkatenda aliyo kufikishieni, mpate kufanikiwa, na muwe mashahidi kwa kaumu zilizo tangulia kwa yaliyo kuja katika Qur'ani kwamba Mitume wao nao walifikisha ujumbe. Na ilivyo kuwa Mwenyezi Mungu amekuchagueni nyinyi khasa kuwa ni wat'iifu kwake, mkashika Sala kwa ukomo wa ukamilifu wake, basi ni waajibu wenu kulipa hayo kwa kumshukuru na kumt'ii, mshike Sala kwa utimilifu wake, na mwape Zaka wanao stahiki, na mumtegemee Mwenyezi Mungu katika mambo yenu yote, na mchukue kwake msaada, kwani Yeye ndiye Msaidizi wenu na ndiye wa kuwanusuru. Yeye ndiye Mbora wa ulinzi na Mbora wa kunusuru.

Sura 23 - Al-Muuminun

Utangulizi

HII NI SURA iliyo teremka Makka. Aya zake ni mia na kumi na nane. Imeanza kwa kuthibitisha mafanikio ya Waumini, na ikafuatia kueleza sifa zao. Kisha ikataja asli ya kuumbwa mwanaadamu, na kubadilika kwake kwa kukua, na kuzalikana vizazi vyake, na baadhi ya mambo yanayo dhihirisha uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tena zikafuatia hadithi za Manabii zinazo fanana kwa umoja wa ujumbe na umoja wa binaadamu, ijapo kuwa watu wanga khitalifiana baina ya wanao kubali na wanao kengeuka. Na sura hii imeeleza khabari za mwenye kutaka uwongofu, na mwenye kupotoka, na msimamo wa washirikina mbele ya Nabii s.a.w. Tena ikaingia kueleza yanayo onekana ya uwezo wa Mwenyezi Mungu katika hukumu za kumuumba mwanaadamu. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* kaingia kuwauliza watu wamjibu kwa kutumia akili zao za maumbile kwa yanayo thibitisha kuwepo kwake, na kuthibitisha Ungu wake. Kisha Sura hii ikaeleza hali za watu itavyo kuwa Siku ya Kiyama, na kwamba wao watahisabiwa, na watafanyiwa uadilifu. Tena Sura inakhitimisha kubainisha Utukufu wake *Subhanahu wa Taa'la*, na kumnabihisha Nabii wake aombe maghira na rehema kutokana na Mbora wa wenye kurehemu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. HAKIKA wamefanikiwa Waumini,¹
2. Ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao,²
3. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi,³
4. Na ambao wanatoa Zaka,⁴
5. Na ambao wanazilinda tupu zao,⁵
6. Isipo kuwa kwa wake zao au kwa iliyo wamiliki mikono yao ya kulia. Kwani hao si wenye kulaumiwa.⁶
7. Lakini anaye taka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka.⁷
8. Na ambao wanazitimiza amana zao na ahadi zao,⁸

1 Kumethibiti kufanikiwa kwa Waumini wanao muamini Mwenyezi Mungu na waliyo kuja nayo Mitume; na wamefuzu kwa wayatakayo.

2 Hao ambao wameambatisha juu ya Imani yao vitendo vyema. Basi hao katika Sala zao humuelekea Mwenyezi Mungu kwa nyoyo zenye kumkhofu na kumnyenyekea, wanahisi unyenyekevu wa mwisho kwake Yeye.

3 Hao wanashughulikia mambo ya maana, wanapuuza vitendo na maneno yasiyo na kheri ndani yake.

4 Nao wanashikilia kutoa Zaka kuwapa wanao stahiki. Kwa hivyo wanakusanya ibada ya mwili na ibada ya mali, na baina ya kujisafisha nafsi na kuyasafisha mali. (Tazama Maelezo 23:4)

5 Nao wanajihifadhi nafsi zao wasiingiane na wanawake. (Tazama Maelezo 23:5)

6 Isipo kuwa kwa njia ya ndoa ya kisharia, au wenye kumiliki masuria. Hao hawalaumiwi. (Tazama Maelezo 23:6)

7 Mwenye kutaka kuingiliana na mwanamke bila ya kupitia njia hizi mbili, basi huyo amevuka mipaka ya sharia hadi ya kuvuka.

8 Na (hao Waumini) wawe ni wenye kuhifadhi kila walicho pewa kuwa ni amana, ikiwa mali au neno au kitendo au chenginecho, na watimize kila ahadi iliyo baina yao na Mwenyezi Mungu au na watu.

9. Na ambao Sala zao wanazihifadhi -⁹

10. Hao ndio warithi,¹⁰

11. Ambao watairithi Pepo ya Firdausi, wadumu humo.¹¹

12. Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo.¹²

13. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti.¹³

14. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwingine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.¹⁴

15. Kisha hakika nyinyi baada ya hayo mtakufa.¹⁵

16. Kisha hakika nyinyi Siku ya Kiyama mtafufuliwa.¹⁶

17. Na kwa yakini tumeziumba juu yenu njia saba. Nasi hatukuwa wenye kughafilika na viumbe.¹⁷

18. Na tumeteremsha kutoka mbinguni maji kwa kiasi na tukayatuliza katika ardhi. Na hakika Sisi tunaweza kuyaondoa.¹⁸

19. Kwa maji hayo tukakufanyieni bustani za mitende na mizabibu, mnapata humo matunda mengi, na katika hayo mnakula;¹⁹

20. Na mti utokao katika mlima wa Sinai, unatoa mafuta na kuwa kitoweo kwa walao.²⁰

Wasikhuni amana, wala wasivunje ahadi.

9 Na wawe wenye kudumisha kutimiza Sala kwa nyakati zake, na kuzitekeleza kwa nguzo zake na unyenyekevu wake, mpaka yapatikane makusudio yake. Nayo ni kuachisha uchafu na maovu.

10 Hawa wenye kusifiwa hivi ndio watakao rithi kheri yote na wataipata Siku ya Kiyama.

11 Hawa ndio Mwenyezi Mungu atawafadhili kwa kuwapa Firdausi, ndio pahala pa juu kabisa huko Peponi, wastarehe humo peke yao.

12 Yawapasa watu waangalie asli ya kuumbwa kwao; kwani hiyo ni dalili za kuonyesha uwezo wetu zenye kupelekea kumuamini Mwenyezi Mungu, na kuamini kufufuliwa. Kwani Sisi tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo.

13 Kisha tukaumba vizazi vyake, navyo ni kuwa tulimfanya mtu kwanza tone ya mbegu ya uzazi - yaani maji yenye kila sifa ya uhai wa mwanzo. Tukaiweka kwenye tumbo la uzazi, napo ni pahala pa utulivu palipo lindwa.

14 Kisha tukaifanya hii mbegu ya manii baada ya kuipandisha na yai la mwanamke kuwa damu. Kisha damu tukaigeuza kuwa kipande cha nyama, kisha tukafanya mafupa, na mafupa tukayavika nyama. Kisha tukatimiza uumbaji wake mwishoe baada ya kuipulizia roho kuwa kiumbe kingine mbali ili kuanza kumjenga. Shani ya Mwenyezi Mungu imetukuka kwa utukufu wake na uwezo wake. Yeye hana mshabaha wake na yeyote katika kuumba kwake na kutengeza kwake na kuanzisha kwake.

15 Kisha hakika nyinyi wanaadamu baada ya haya mambo yenu tuliyo yataja ni wenye kuyaendea mauti bila ya shaka yoyote.

16 Na kisha nyinyi mtafufuliwa Siku ya Kiyama kwa ajili ya kuhisabiwa na kulipwa jaza yenu.

17 Na hakika Sisi tumeziumba mbingu saba zilizo nyanyuka juu yenu. Ndani yake vipo viumbe ambavyo hatukughafilika navyo. Tunavihifadhi na tunaviendesha. Na Sisi kabisa hatughafiliki na viumbe vyote vyote. Bali tunavilinda visipotee na kuharibika, na tunavipangia mambo yao yote kwa hikima. (*Tazama Maelezo 23:17*)

18 Na Sisi tumeteremsha kutoka mbinguni mvua kwa hikima na kipimo katika umbo lake na kuteremka kwake. Na kusahilisha kwa ajili ya manufaa tumeijaalia ikae juu ya uso wa ardhi na ndani yake chini. Na Sisi hakika ni wenye kuweza kuiondoa wasipate kunafiika nayo. Lakini hatukufanya hayo kwa kukuoneeni huruma. Basi muaminini Mwenye kuiumba na mumshukuru. (*Tazama Maelezo 23:18*)

19 Kwa haya maji tukakuumbieni mabustani ya mitende na mizabibu yenye matunda mengi kwa ajili yenu, na katika hayo nyinyi mnakula.

20 Na tumekuumbieni mti wa zaituni unao ota katika jimbo la Mlima wa Sinai. Katika matunda yake yanapatikana mafuta yanayo kufaeni. Na hizo zaituni ni kitoweo cha chakula kwa wanao kula. (*Tazama*

21. Na hakika mnayo mazingatio makubwa katika nyama hoa - tunakunywesheni katika vile viliomo matumboni mwao, na nyinyi mnapata katika hao manufaa mengi, na pia mnawala.²¹
22. Na juu yao na juu ya marikebu mnabebwa.²²
23. Na hakika tulimtuma Nuhu kwa watu wake, akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mungu asiye kuwa Yeye. Basi je! Hamwogopi?²³
24. Walisema wale wakuu walio kufuru katika watu wake: Huyu si chochote ila ni mtu tu kama nyinyi. Anataka kujipa ubora juu yenu. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu amependa basi yakini angeli teremsha Malaika. Hatukusikia haya kwa baba zetu wa zamani.²⁴
25. Huyu si lolote ila ni mtu mwenye wazimu. Basi mngojeeni tu kwa muda.²⁵
26. Akasema (Nuhu): Mola wangu Mlezi! Ninusuru kwa kuwa wamenikanusha.²⁶
27. Tukampa wahyi: Unda jahazi mbele ya macho yetu na uwongozi wetu! Basi itapo fika amri yetu na ikafurika tanuri, hapo waingize ndani yake wa kila namna dume na jike, na ahali zako, isipo kuwa yule ambaye katika wao juu yake imekwisha tangulia kauli. Wala usinitajie hao walio dhulumu. Kwani hao bila ya shaka watazamishwa.²⁷
28. Basi utakapo tulia wewe na walio pamoja nawe humo marikebuni, sema: *Alhamdulillah* Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, aliye tuokoa na watu madhaalimu!²⁸

Maelezo 23:20)

21 Na nyinyi mnapata kutokana na nyama hoa, nyama wa kufuga, nao ni ngamia, ng'ombe, kondoo na mbuzi, mambo yanayo onyesha uwezo wetu na fadhila zetu juu yenu kwa kukuneemesheni. Tunakunywesheni kutoka matumboni mwao maziwa safi, matamu, mepesi kwa wenye kuyanywa. Na mbali ya maziwa mnapata manufaa mengine kama nyama, na sufi, na manyoya. Na kutokana na hao nyinyi mnaishi na mnaruzukiwa.

22 Na juu ya hawa wanyama wa kufuga na marikebu nyinyi mnapanda, na mnapakia mizigo. Basi Sisi tumekuumbieni njia za usafirishaji na upakizi nchi kavu na baharini. Na kwa hizo mnapata kuwasiliana nyinyi kwa nyinyi.

23 Na katika visa vya watu wa kale pana mazingatio kwa ajili yenu mpate kuamini. Basi Sisi tulimtuma Nuhu kwa watu wake, naye akawaambia: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu pekee. Kwani nyinyi hamna anaye stahiki kuabudiwa asiye kuwa Yeye. Hamwogopi adhabu yake, na kuondoka neema zake mkiimuasi?

24 Wakubwa wa kaumu yake walio kufuru wakiukanya wito wake na wakizuia watu wasimfuata, walisema: Hapana khitilafu yoyote baina ya Nuhu na nyinyi. Kwani yeye ni mtu kama nyinyi, lakini anataka kujipa ubora juu yenu kwa huu wito wake. Na lau kuwa wapo Mitume wanao toka kwa Mwenyezi Mungu kama anavyo dai yeye, basi ange waletea Malaika. Sisi hatukupata kusikia wito huu katika taarikhi za baba zetu walio tangulia, wala kutumwa binaadamu kuwa ni Mtume.

25 Huyu si chochote ila ni mtu mwenye wazimu. Na kwa hivyo wakasema: Ngojeni, na mstahamilieni mpaka ukashifike wazimu wake, au kufike kuangamia kwake.

26 Nuhu akamwomba Mola wake Mlezi baada ya kukata tamaa kuamini kwao, akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ninusuru nao, na watie adabu kwa sababu ya kuukadhibisha kwao wito wangu!

27 Tukamwambia kwa njia ya ufunuo (wahyi): Unda jahazi, nawe utalindwa na uangalizi wetu. Shari yao haitokupata, nasi tutakuongoza katika kazi yako. Na ikifikilia miadi ya kuwaadhibu, na ukaona tanuri inafoka maji kwa amri yetu, basi waingize katika jahazi katika kila namna ya viumbe vilivyo hai dume na jike. Na waingize ahali zako, isipo kuwa walio kwisha thibitika adhabu yao kwa kukosa kwao Imani. Wala usiniombe kuwaokoa wale walio dhulumu nafsi zao na wakawadhulumu na wengineo kwa ukafiri na uasi. Kwani Mimi nimewahukumia kuwazamisha kwa sababu ya dhulma yao ya ushirikina na uasi. (Tazama Maelezo 23:27)

28 Na ukisha panda na ukatua wewe na walio pamoja nawe katika jahazi hiyo basi sema kwa kumshukuru Mola wako Mlezi: *Alhamdulillah*! Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ndiye aliye tuokoa

29. Na sema: Mola wangu Mlezi! Niteremshe mteremsho wenye baraka, na Wewe ni Mbora wa wateremshaji.²⁹
30. Hakika katika hayo yapo mazingatio. Na kwa yakini Sisi ni wenye kuwafanyia mitihani.³⁰
31. Kisha baada yao tukaanzisha kizazi kingine.³¹
32. Tukawapelekea Mtume miongoni mwao, kuwaambia: Muabuduni Mwenyezi Mungu! Hamna mungu asiye kuwa Yeye. Jee, hamwogopi?³²
33. Na wakubwa katika watu wake walio kufuru na wakakanusha mkutano wa Akhera, na tukawadekeza kwa starehe katika maisha ya dunia, walisema: Huyu si chochote ila ni binaadamu kama nyinyi; anakula mlacho, na anakunywa mnywacho.³³
34. Na nyinyi mkimt'ii mtu kama nyinyi basi hakika mtakuwa khasarani.³⁴
35. Hivyo anakuahidini ati ya kwamba mtakapo kufa na mkawa udongo na mifupa kuwa mtatolewa?³⁵
36. Hayawi! Hayawi hayo mnayo ahidiwa.³⁶
37. Hapana ila uhai wetu wa duniani tu, tunakufa na kuishi basi. Wala sisi hatutafufuliwa.³⁷
38. Huyu si lolote ila ni mtu anaye mzulia Mwenyezi Mungu uwongo, wala sisi sio wa kumuamini.³⁸
39. Akasema: Mola wangu Mlezi! Ninusuru kwa sababu wanarikanusha.³⁹
40. (Mwenyezi Mungu) akasema: Baada ya muda mchache watakuwa wenye kujuta.⁴⁰

na shari ya watu makafiri walio asi.

29 Na useme: Ewe Mola Mlezi! Nijaalie nishuke mashukio yenye baraka, pahala pazuri pa kukaa wakati wa kuteremka nchi kavu. Na unitunukie amani hapo. Kwani ni Wewe tu peke yako unaye weza kututeremsha pahala pa kheri na amani na salama.

30 Hakika katika kisa hichi yapo mazingatio na mawaidha mengi. Na hakika Sisi tunawajaribu (tunawapa mitihani) waja wetu kwa kheri na shari. Na ndani ya nafsi zao wana utayarisho wa yote hayo.

31 Tena baada ya kaumu ya Nuhu tukaumba namna ya watu wengine, na wao ni A'adi.

32 Tukawapelekea Huud. Naye ni katika wao. Tukawaambia kwa ulimi wake: Muabuduni Mwenyezi Mungu peke yake. Kwani nyinyi hamna Mungu anaye stahiki kuabudiwa asiye kuwa Yeye. Ni Yeye peke yake anaye faa mumwogope. Basi, jee mmeikhofu adhabu yake mkimuasi?

33 Na wakubwa katika kaumu yake walio kufuru na kukadhibisha kukutana na Mwenyezi Mungu na mambo ya Akhera ya hisabu na malipo, na tukawapa sehemu kubwa ya starehe na neema, wakasema kwa kukanusha wito wake, na kuwazuia watu wasimfuate: Hapana khitilafu yo yote baina ya Huud na nyinyi. Anakula chakula hicho hicho mnacho kila nyinyi. Na anakunywa vinywaji hivyo hivyo mnavo vinywa nyinyi. Mfano wa huyu hawezi kuwa Mtume, kwa sababu hana sifa msizo kuwa nazo nyinyi.

34 Na wakawahadharisha kwa nguvu na mkazo, wakiwaambia: Mkimt'ii mtu aliye kama nyinyi kwa utu wake, basi nyinyi hakika mtakuwa mmekhasiri kwa kuwa hamtapata manufaa yo yote mkimfuata.

35 Wakawaambia pia katika kukanya kufufuliwa: Hivyo Huud anakuahidini kuwa mtafufuliwa kutoka makaburini kwenu baada ya kwisha kufa kwenu, na mkawa udongo na mafupa yasiyo kuwa na nyama na mishipa.

36 Hayo anayo kuahidini ni ya mbali mno, wala hayatakuwa abadan.

37 Hapana uhai ila mmoja tu. Nao ndio huu uhai wa duniani, ambao tunauona una mauti na uhai unao tupitia. Kinacho zaliwa kinazaliwa, na kilicho hai kinakufa. Wala hatutofufuliwa baada ya kwisha kufa kabisa.

38 Huyu si chochote ila ni mtu aliye mzulia Mwenyezi Mungu, na akadai kwamba Mwenyezi Mungu kamtuma yeye. Na amesema uwongo katika hayo anayo tuitia. Wala hatutomsadiki abadan.

39 Huud akasema baada ya kwisha kata tamaa kuamini kwao: Ewe Mola wangu Mlezi! Ninusuru na uwatie adabu, kwa sababu ya kuukadhibisha wito wangu.

40 Mwenyezi Mungu akamwambia Huud kuzidi kutilia nguvu ahadi yake: Baada ya muda mchache

41. Basi ukawanyakua ukelele kwa haki, na tukawafanya kama takataka zinazo elea juu ya maji. Ikapotelea mbali kaumu ya madhaalimu!⁴¹
42. Kisha tukaleta baada yao vizazi vingine.⁴²
43. Hapana umma uwezao kutanguliza ajali yake wala kuikawiza.⁴³
44. Kisha tukawatuma Mitume wetu, mmoja baada ya mmoja. Kila umma alipo wafikia Mtume wao walimkanusha. Tukawafuatanisha hawa baada ya hawa, na tukawafanya ni hadithi za kusimuliwa. Wakapotelea mbali watu wasio amini.⁴⁴
45. Kisha tukamtuma Musa na nduguye, Haaruni, pamoja na ishara zetu na hoja zilizo wazi.⁴⁵
46. Kumwendea Firauni na wakuu wake. Lakini walijivuna, nao walikuwa watu majeuri.⁴⁶
47. Wakasema: Je, tuwaamini wanaadamu wawili hawa kama sisi, na ambao watu wao ni watumwa wetu?⁴⁷
48. Basi wakawakanusha, na wakawa miongoni mwa walio angamizwa.⁴⁸
49. Na hakika tulimpa Musa Kitabu ili wapate kuongoka.⁴⁹
50. Na tukamfanya mwana wa Mariamu na mama yake kuwa ni Ishara, na tukawapa makimbilio kwenda mahali palipo inuka penye utulivu na chemchem za maji.⁵⁰
51. Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa mnayo yatenda.⁵¹
52. Na kwa yakini huu Umma wenu ni Umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi nicheni Mimi.⁵²

watakuja juta, kwa waliyo yafanya, itapo wateremkia adhabu.

41 Ukawachukua ukelele mkali ulio wahilikisha kama walivyo stahiki. Tukawafanya kwa udhalili na udhaifu kama vijiti na majani ya miti yanayo chukuliwa na maji ya mvua. Na huko ni kuteketea na kupotelea mbali na rehema kwa madhaalimu kwa ukafiri wao na uasi wao.

42 Kisha baada yao tukawaumba kaumu nyengine wasio kuwa wao, kama kaumu ya Saleh na ya Luut'i na ya Shuaib.

43 Kila umma una zama zake maalumu, hazitangulii wala hazikawii.

44 Kisha tukawatuma Mitume wetu wakifuatana, kila mmoja kwa kaumu yake. Kila akija Mtume kwa kaumu yake waliukadhibisha wito wake. Nasi tukawateketeza mfululizo, na tukazifanya khabari zao ni hadithi za watu kusimuliana na kuzistaajabia. Basi hao kaumu wasio isadiki Haki wala hawafuati wametengeka mbali na rehema, na wamehiliki.

45 Kisha tukamtuma Musa na nduguye, Haaruni, tukawapa dalili za kukata kuthibitisha ukweli wa ujumbe wao, na hoja wazi yenye kudhihirisha kuwa wao ni kweli wametumwa kutoka kwangu.

46 Tuliwatuma wawili hao kwa Firauni na kaumu yake. Wakakataa kuamini kwa ajili ya takaburi, na wao ni watu walio kuwa wakisifika kwa kiburi, na majivuno, na ujeuri.

47 Wakasema kwa mastajabu na kukanya: Je, tuuamini wito wa watu wawili walio ni wanaadamu kama sisi, na tena watu wao hawa Wana wa Israili ni wenye kutunyenyekea sisi na kutut'ii kama ni watumwa?

48 Basi waliwafanya waongo katika huo wito wao, na wakawa wenye kuhiliki kwa kuzamishwa.

49 Na hakika tulimfunulia Musa Taurati apate kuwaongoa watu wake kwa yaliyomo ndani yake ya uwongozi kwendea hukumu na njia za mafanikio.

50 Na tumemjaalia Isa bin Maryamu na mama yake, kwa vile kuchukua mimba bila ya kuingiliwa na mtu, na kuzaliwa yeye Isa bila ya baba, kuwa dalili ya kukata ya uwezo wetu wenye kushinda. Na tukamweka Maryamu pahala pa kukaa penye ardhi iliyo nyanyuka na kukunjuka panapo faa kukaa, na pana maji mengi. Na hayo ndiyo yanayo wezesha maisha ya starehe.

51 Tumewaambia Mitume wawafikishie watu wao: Kuleni vyakula vya kila namna vya halali na vizuri, na stareheni na ishukuruni neema yangu kwa vitendo vyema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa myatendayo na nitakulipeni kwayo.

52 Na tukawaambia wawafikishie watu wao: Hakika hii Dini niliyo kutumeni muifikishe ni Dini moja

53. Lakini walikatiana jambo lao mapande mbali mbali. Kila kundi likifurahia kwa waliyo nayo.⁵³
54. Basi waache katika ghafla yao kwa muda.⁵⁴
55. Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile tunavyo wapa mali na watoto⁵⁵
56. Ndio tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.⁵⁶
57. Kwa hakika hao ambao kwa kumwogopa Mola wao Mlezi wananyenyekea,⁵⁷
58. Na wale ambao Ishara za Mola wao Mlezi wanaziamini,⁵⁸
59. Na wale ambao Mola wao Mlezi hawamshirikishi,⁵⁹
60. Na wale ambao wanatoa walicho pewa, na hali nyoyo zao zinagopa kwa kuwa watarejea kwa Mola wao Mlezi,⁶⁰
61. Basi wote hao ndio kimbilia katika mambo ya kheri, na ndio watakao tangulia kuyafikia.⁶¹
62. Na hatuilazimishi nafsi ila kwa kadri ya uwezo wake. Na tunacho kitabu kisemacho kweli. Nao hawatadhulumiwa.⁶²
63. Lakini nyoyo zao zimeghafilika na hayo, na wanavyo vitendo vinginevyo wanavyo vifanya.⁶³
64. Hata tutakapo watia katika adhabu wale walio dekezwa kwa starehe kati yao, hapo ndipo watapo yayatika.⁶⁴

kwa mintarafu ya Imani na misingi ya sharia. Na hakika nyinyi ni umma mmoja katika vizazi vyote. Miongoni mwao wapo walio ongoka, na wapo walio potoka. Na Mimi ndiye Mola wenu Mlezi niliye kuamrisheni muifuata, basi iogopeni adhabu yangu pindi mkiasi.

53 Lakini watu walilikata kata hili jambo la Dini yao. Wapo kati yao walio ongoka, na wapo walio potoka ambao wakafuata matamano yao, wakafarikiana kwa sababu hiyo wakawa makundi mbali mbali yenye kufanyiana uadui. Kila kikundi kinafurahi kwa walio nayo, kwa kudhania kuwa wao tu ndio walio sibu.

54 Basi, ewe Muhammad, waachilie mbali makafiri na ujinga wao na kughafilika kwao, maadamu wewe umekwisha wanasih, mpaka Mwenyezi Mungu awahukumie adhabu baadae.

55 Hivyo hawa waasi wanadhani ya kwamba pale Sisi tunapo wawacha wakistarehe na mali na watoto tulio wapa

56 Ndio basi Sisi tumekuwa radhi nao, na kheri zikawamiminikia mbio mbio na kwa wingi? Hao ni kama wanyama, hawatambui, kwa kuwa hawazitumii akili zao. Mimi si radhi nao. Na hizi neema ni kuwapururia tu, kuwapa muda.

57 Hakika wale ambao humkhofu Mwenyezi Mungu na humwogopa, na zimejaa ndani yao khofu ya Mwenyewe *Subhanahu*,

58 Na wale ambao wanaziamini Ishara za Mola wao Mlezi ziliomo ulimwenguni na zinazo somwa katika Kitabu kilicho teremshwa,

59 Na wale ambao hawamshirikishi Mwenyezi Mungu na yeyote,

60 Na wale ambao wanatoa katika vile anavyo waruzuku Mwenyezi Mungu, na wanafanya a'mali yao na hali wao wana khofu wasifanye taksiri, kwa sababu bila ya shaka wao ni wenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu kwa kufufuliwa na watahisabiwa,

61 Hao wote hukimbilia na a'mali zao kuendea kupata kheri, na wao ni wenye kuwatangulia wengineo katika kupata huko.

62 Na Sisi hatumlazimishi mtu yeyote ila kwa analo liweza kulifanya, kwa sababu limo ndani ya makdara yake. Na kila a'mali katika a'mali za waja zimesajiliwa kwetu katika kitabu, na tutawapa khabari zake kama zilivyo. Na wao hawatadhulumiwa kwa kuongezewa adhabu wala kupunguziwa thawabu.

63 Lakini makafiri kwa sababu ya inadi yao na chuki zao ni wenye kughafilika na kufanya kheri, na kujikalifu kufanya liwezekanalo, na kwamba kuna hisabu ya kuchungua kila kitu. Na mbali na hayo bado wanavyo vitendo vingine viovu wanavyo dumu navyo.

64 Na Sisi tunapo wapatiliza adhabu matajiri wenye kudeka katika starehe zao hupiga makelele na wakayayatika kuomba msaada.

65. Msiyatike leo! Hakika nyinyi hamtanusurika nasi.⁶⁵
66. Hakika zilikuwa Aya zangu mkisomewa, nanyi mkirudi nyuma juu ya visigino vyenu,⁶⁶
67. Na huku mkitakabari na usiku mkiizungumza (Qur'ani) kwa dharau.⁶⁷
68. Je, hawakuifikiri kauli, au yamewajia yasiyo wafikia baba zao wa zamani?⁶⁸
69. Au hawakumjua Mtume wao, ndio maana wanamkataa?⁶⁹
70. Au wanasema: Ana wazimu? Bali amewajia kwa Haki, na wengi wao wanaichukia Haki.⁷⁰
71. Na lau kuwa Haki ingeli fuata matamano yao, basi zingeli haribika mbingu na ardhi na waliomo ndani. Bali tumewaletea ukumbusho wao, nao wanajitenga mbali na ukumbusho wao.⁷¹
72. Au unawaomba ujira? Lakini ujira wa Mola wako Mlezi ni bora, na Yeye ndiye Mbora wa wanao ruzuku.⁷²
73. Na kwa yakini wewe unawaita kwenye Njia Iliyo Nyooka.⁷³
74. Na hakika wale wasio iamini Akhera wanajitenga na Njia hiyo.⁷⁴
75. Na lau tungeli warehemu na tukawaondolea shida waliyo nayo bila ya shaka wangeli endelea katika upotofu wao vile vile, wakitangatanga.⁷⁵
76. Na hakika tuliwatia adhabu kali; lakini hawakuelekea kwa Mola wao Mlezi wala hawakunyenyeka.⁷⁶

65 Basi tunawaambia: Msiyatike, wala msiombe msaada hivi sasa. Hamtatoka ndani ya adhabu yangu, wala kuyayatika kwenu hakufai kitu.

66 Hamna udhuru. Kwani Aya zangu zenye kuteremshwa kwa wahyi zilikuwa mkisomewa, nanyi mkizipuza kwa mapuza yenye kugeuza hali zenu, na wala hamkuzisadiki, wala hamkuzifuata kwa vitendo.

67 Na nyinyi katika mapuza yenu mlikuwa mnatakabari na mnafanyia maskhara, mkiutaja huu Wahyi kwa sifa mbaya mnapo kutana katika taanusi zenu za usiku.

68 Je! Hawa wenye kupuza wamekuwa wajinga hata hawakuizingatia Qur'ani wakaijua kwamba hii hakika ni Haki? Au huu wito wa Muhammad kwao umekuwa ni namna mbali kuliko walio kuja nayo Mitume wengine kwa kaumu zilizo kwisha tangulia walio ambao baba zao waliwawahi?

69 Au hawamjui Mtume wao Muhammad aliye kulia kati yao katika tabia zake tukufu ambazo hazijapata kuwa na uwongo, na wao hivi sasa wanaukataa wito wake kwa dhulma na husda.

70 Au wanasema kuwa huyu ni mwendawazimu? Hasha! Huyu hakika kawaletea Dini ya Haki, na wengi wao wanaichukia haki, kwani hiyo ni kinyume na matamano yao na mapenzi yao, basi kwa hivyo hawamuamini.

71 Ingeli kuwa Haki inafuata matamano yao ufisadi ungeli enea ulimwenguni, na hawa za nafsi zingeli pambana wenyewe kwa wenyewe. Lakini Sisi tumewapelekea Qur'ani ambayo inawakumbusha haki ambayo inapasa wote wajumuike juu yake. Na juu ya hivyo wao wanayapuza hayo. (*Tazama Maelezo 23:71*)

72 Kwani, ewe Nabii! Unawataka ujira kwa huku kufikisha kwako ujumbe? Hayakuwa hayo! Kwa kuwa hakika ujira wa Mola wako Mlezi ni bora zaidi kuliko walio nao wao; na Yeye ndiye Mbora wa kutoa.

73 Na hakika wewe, ewe Muhammad, hapana shaka yoyote unawaitia Dini ambayo ndiyo Njia Iliyo Nyooka yenye kupelekea Uwokovu.

74 Na hakika hao wasio iamini Akhera na yalioko huko ya Pepo au Moto wanaiacha Njia Iliyo Nyooka inayo mhifadhi mpitaji wakaishika njia ya ubabaishi na misukosuko na ufisadi.

75 Na lau tungeli warehemu, na tukawaondolea madhara yalio wateremkia katika miili yao, na ukame katika mali yao, na mfano wa hayo, basi hapana shaka yoyote wangeli zidi ukafiri, na wakaendelea katika maasi na jeuri.

76 Na Sisi kwa hakika tuliwapa adhabu kama kwa kuwauwa au kuwaletea njaa. Na wala hawakunyenyeka Mola wao Mlezi, bali waliendelea na jeuri zao na kiburi chao kiasi ya kuondoka tu hiyo adhabu.

77. Mpaka tulipo wafungulia mlango wa adhabu kali, hapo ndipo wakawa wenye kukata tamaa.⁷⁷
78. Na Yeye ndiye aliye kuumbieni kusikia na kuona na nyoyo za kufahamu. Ni kuchache mno kushukuru kwenu.⁷⁸
79. Na Yeye ndiye aliye kuenezeni katika ardhi, na kwake Yeye mtakusanywa.⁷⁹
80. Na Yeye ndiye anaye huisha na kufisha, na yake Yeye mabadiliko ya usiku na mchana. Basi je! Hamfahamu?⁸⁰
81. Bali wanasema kama walivyo sema watu wa kwanza.⁸¹
82. Walisema: Je! Tukisha kufa tukawa udongo na mifupa ndio tutafufuliwa?⁸²
83. Tuliahidiwa haya sisi na baba zetu zamani. Hayakuwa haya ila ni visa vya uwongo vya watu wa zamani.⁸³
84. Sema: Ni ya nani ardhi na viliomo ndani yake, kama nyinyi mnajua?⁸⁴
85. Watasema: Ni vya Mwenyezi Mungu! Sema: Basi, je, hamkumbuki?⁸⁵
86. Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa A'rshi Kuu?⁸⁶
87. Watasema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Sema: Basi je, hamwogopi?⁸⁷
88. Sema: Ni nani mkononi mwake umo Ufalme wa kila kitu, naye ndiye anaye linda, wala hakilindwi asicho taka, kama mnajua?⁸⁸
89. Watasema: (Ufalme huo) ni wa Mwenyezi Mungu. Sema: Basi vipi mnadanganyika?⁸⁹

77 Wanashikilia kupuuzwa kwao mpaka pale tunapo wapatiliza kwa adhabu kali ya njaa au mauwaji hapa duniani huwa tena wanababaika na kukata tamaa, hawaioni njia ya kuvuka.

78 Na yawaje mkamkufuru Mwenyezi Mungu na hali ni Yeye ndiye aliye kuumbieni usikizi mkaisikia Haki, aliye kupeni uwezo wa kuona mkauona ulimwengu na viliomo ndani yake, na akakupeni akili mzingatie kwayo utukufu wake mpate kuamini? Hakika nyinyi hamumshukuru Mwenye kuumba vyote hivyo kwa Imani na ut'iifu ila kwa uchache tu, nao ni uchache mno!

79 Na Yeye ndiye aliye kuumbeni duniani, na kwake Yeye peke yake ndio mtarejeshwa Siku ya Kiyama kwa ajili ya malipo.

80 Na Yeye ndiye anaye huisha na kufisha, na kwa amri yake na sharia zake ndio usiku na mchana zinapitishana. Na kukhitalifiana kwazo kwa urefu na ufupi, hamzingatii hiyo kuwa ni dalili ya uwezo wake na kupasa kumuamini Yeye na kuamini kufufuliwa? (*Tazama Maelezo 23:80*)

81 Hawakuzingatia hayo, bali waliwafuata wakanushaji walio kwisha tangulia, wakasema kama walivyo sema hao.

82 Katika kukanusha kwao kufufuliwa, walisema: Hivyo sisi tutafufuliwa baada ya kwisha geuka mchanga na mifupa?

83 Sisi tuliahidiwa haya, na pia baba zetu waliahidiwa hayo hapo zamani. Haya si chochote ila ni ahadi za uwongo walizo buni watu wa zamani.

84 Ewe Muhammad! Waambie: Ni nani aliye imiliki ardhi na viliomo ndani yake, tangu watu mpaka viumbe vyote? Kama nyinyi mna ujuzi nijibuni.

85 Watakiri kuwa ardhi ni ya Mwenyezi Mungu. Basi hapo tena waambie: Hamkumbuki kuwa Mwenye kumiliki hayo ndiye anaye faa kuabudiwa peke yake?

86 Waambie tena: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa A'rshi Kuu? (Kiti Kikuu cha Enzi)

87 Watakiri kuwa huyo ni Mwenyezi Mungu. Basi waambie: Je! Hamwogopi matokeo ya ushirikina wenu na ukafiri wenu na kumuasi kwenu Mwenye uumbaji huu wote mkubwa?

88 Waambie vile vile: Nani mwenye ufalme wa kila kitu mkononi mwake, na mwenye madaraka yasio na ukomo katika kila kitu, na ambaye ndiye kwa uwezo wake analinda kila kitu, wala hayamkiniki yeyote kumlinda yeyote na adhabu yake? Kama nyinyi mnajua jawabu, basi nijibuni.

89 Watakiri kuwa hakika huyo ni Mwenyezi Mungu. Waambie: Basi huwaje mkadanganyika kwa pumbao na kuchochewa na mashetani, na mkaacha ut'iifu wa Mwenyezi Mungu?

90. Bali tumewaleta Haki, na kwa yakini hao ni waongo.⁹⁰
91. Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umbra, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepekana na sifa wanazo msifu.⁹¹
92. Mjuzi wa siri na dhaahiri, na ametukuka juu ya hayo wanayo mshirikisha nayo.⁹²
93. Sema: Mola wangu Mlezi! Ukinionyesha adhabu waliyo ahidiwa,⁹³
94. Mola wangu Mlezi! Usinijaalie katika watu madhaalimu hao.⁹⁴
95. Na hakika Sisi ni waweza wa kukuonyesha tuliyo waahidi.⁹⁵
96. Kinga maovu kwa kutenda yaliyo mema zaidi. Sisi tunajua wayasemayo.⁹⁶
97. Na sema: Mola wangu Mlezi! Najikinga kwako na wasiwasi wa mashet'ani.⁹⁷
98. Na najikinga kwako, Mola wangu Mlezi, wasinikaribie.⁹⁸
99. Mpaka yanapo mfikia mmoja wao mauti, husema: Mola wangu Mlezi! Nirudishe.⁹⁹
100. Ili nitende mema sasa badala ya yale niliyo yaacha. Wapi! Hii ni kauli aisemayo yeye tu. Na nyuma yao kipo kizuizi mpaka siku watapo fufuliwa.¹⁰⁰
101. Basi litapo pulizwa baragumu hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana.¹⁰¹
102. Ama wale ambao mizani zao zitakuwa nzito, hao ndio wenye kufanikiwa.¹⁰²
103. Na wale ambao mizani zao zitakuwa nyepesi, hao ndio walio zitia khasarani nafsi

90 Hakika Sisi tumewabainishia Haki kwa ndimi za Mitume, na wao ni waongo katika kila jambo linalo khitalifu na Haki hii.

91 Mwenyezi Mungu hakumchukua yeyote kuwa ni mwanawe. Yeye ametakasika na hayo. Wala hana mshirika. Angeli kuwa na mshirika basi kila mmoja wao angejipa madaraka ya pekee kwa alivyo viumba, na vikawa ndio milki yake, na wangeli gombana wenyewe kwa wenyewe kama wanavyo onekana wafalme wanavyo fanya. Na ulimwengu ungeli fisidika kwa mizozano hiyo. Basi Mwenyezi Mungu ametakasika na hayo wayasemayo washirikina yanayo kwenda kinyume na Haki.

92 Na Yeye amevizunguka vitu vyote kwa kuvijua. Anajua tusiyo yaona na tunayo yaona. Mwenyezi Mungu ametakasika na hayo wanayo mnasibisha nayo makafiri kuwa ati ana washirika.

93 Ewe Nabii! Sema: Ukiwateremshia adhabu ulio waahidi hapa duniani nami nipo pamoja nao.

94 Basi nakuomba usinifanye mwenye kuadhibiwa pamoja na makafiri waasi.

95 Na Sisi tunaweza kwa utimilivu kukuonyesha adhabu tulio waahidi ikiwateremkia. Basi wewe tuwa ujue kuwa tutashinda.

96 Wewe endelea na wito wako, na ukabili uovu wao kwa vitendo vilivyo vizuri kama kusamehe au vyenginevyo. Na Sisi tunajua vyema wanakutaja vipi wewe, na wanavyo usema kwa ubaya huo wito wako kwa uwovu na uzushi. Na Sisi tutawalipa kwa hayo.

97 Nawe sema: Ewe Mola Mlezi! Najilinda kwako na wasiwasi wa mashetani wasiniingilie katika nafsi yangu kwa vitendo visio kupendeza.

98 Na ewe Mola Mlezi! Najilinda kwako wasiwe nami katika kitendo chochote ili kitendo hicho kiwe kimetakasika, safi, kwa ajili ya ridhaa yako tukufu

99 Wanaendelea kuwakanusha mpaka utapo fika wakati wa kufa mmoja wao hujuta na akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nirudishe duniani.

100 Ili nipate kufanya a'mali njema katika mali au wakati nilio acha. Wala ombi lake halitokubaliwa. Kwani haya ni maneno anayasema bila ya faida, hayakubaliwi. Na pindi akikubaliwa hatotenda kitu. Na juu ya yote hatorudi kabisa! Kwani mauti ni kizuizi baina yao na hayo wanayo yatamani mpaka Mwenyezi Mungu atapo wafufua.

101 Ukifika wakati wa kufufuliwa tutawafufua kutoka makaburini kwao. Na hayo ni kwa mfano wa kupulizwa tarumbeta watafufuka nao wamefarikiana. Hapana mtu utaomfaa ujamaa wake na fulani. (Ujamaa Kiswahili maana yake makhusiano ya nasaba, sio usoshalisti.) Wala hapana mtu atae muomba mtu kitu cha kumfaa. Kwani kila mmoja wao siku hiyo atakuwa kashughulika na lake.

102 A'mali (Vitendo) ndio mizani ya kupimia. Mwenye Imani nzuri na vitendo vyema atakuwa na uzito katika mizani ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio walio fuzu.

zao, na katika Jahannamu watadumu.¹⁰³

104. Moto utababua nyuso zao, nao watakuwa na nyuso zilizo kunjana.¹⁰⁴

105. Je! Hazikuwa Aya zangu mkisomewa, na nyinyi mkizikanusha?¹⁰⁵

106. Watasema: Mola wetu Mlezi! Tulizidiwa na uovu wetu na tukawa watu tulio potea.¹⁰⁶

107. Mola wetu Mlezi! Tutoe humu Motoni. Na tufanyapo tena basi kweli sisi ni wenye kudhulumu.¹⁰⁷

108. Atasema Mwenyezi Mungu: Tokomeeni humo, wala msinisemeze.¹⁰⁸

109. Bila ya shaka lilikuwapo kundi katika waja wangu likisema: Mola wetu Mlezi! Tumeamini; basi tusamehe na uturehemu, nawe ndiwe Mbora wa wanao rehemu.¹⁰⁹

110. Lakini nyinyi mliwakejeli hata wakakusahaulisheni kunikumbuka, na mlikuwa mkiwacheka.¹¹⁰

111. Hakika Mimi leo nimewalipa kwa vile walivyo subiri. Bila ya shaka hao ndio wenye kufuzu.¹¹¹

112. Atasema: Mlikaa muda gani katika ardhi kwa hisabu ya miaka?¹¹²

113. Watasema: Tulikaa siku moja au sehemu ya siku. Basi waulize wanao weka hisabu.¹¹³

114. Atasema: Nyinyi hamkukaa huko duniani ila kidogo, laiti ingeli kuwa mnajua.¹¹⁴

115. Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?¹¹⁵

116. Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki, hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi Tukufu.¹¹⁶

103 Na asiye kuwa na thawabu au vitendo vyenye uzito mbele ya Mwenyezi Mungu, hao ndio walio zikhasiri nafsi zao kwa kuziiza kwa Shetani. Nao wataadhibiwa Motoni, wadumu humo.

104 Moto utawababua nyuso zao, nazo zitakuwa zimekunjana kwa uwovu wa mwisho wao.

105 Mwenyezi Mungu anawakemea na anawaambia: Aya zangu zilizo kuwa zinateremshwa zilikuwa mkisomewa duniani, nanyi mkizikadhibisha.

106 Watasema nao wanakiri makosa yao : Ewe Mola wetu Mlezi! Maasi yetu yalikuwa mengi, ndio yakatupatia mashaka, na tukawa wenye kupotea tukaiacha njia ya sawa.

107 Na watasema: Mola wetu Mlezi! Tutoe Motoni na uturejeshe duniani. Basi tukirudi tena kwenye ukafiri na uasi basi tutakuwa kweli ni twenye kujidhulumu nafsi zetu.

108 Na Mwenyezi Mungu atawaambia kwa kuwadharau na kuwabeza: Kaeni humo kwa madhila na unyonge, wala msiseme nami kabisa!

109 Mimi sikukudhulumuni, bali nyinyi mmejidhulumu wenyewe. Kwani Waumini wema katika waja wangu walikuwa wakisema duniani: Ewe Mola wetu Mlezi! Tumeamini. Basi tughufirie na uturehemu. Na Wewe ndiwe Mbora wa wanao rehemu.

110 Na nyinyi daima mlikuwa mkiwafanyia maskhara, mpaka maskhara yenu yakakusahaulisheni kunikumbuka Mimi na kuniabudu Mimi. Basi hamkuamini wala hamkut'ii. Nanyi mlikuwa mkiwacheka kwa kejeli.

111 Hakika Mimi hii leo nimewalipa wao kwa mafanikio, kwa kuwa waliyavumilia maskhara yenu na maudhi yenu.

112 Mwenyezi Mungu atawaambia makafiri: Mliishi miaka mingapi huko duniani?

113 Watasema kwa kuyaona mafupi maisha yao kwa adhabu wanayo ikuta: Tuliishi muda wa siku moja au baadhi ya siku hivi. Basi waulize wanao weza kuhisabu, sisi tumeshughulishwa na hii adhabu.

114 Basi Mwenyezi Mungu atawaambia: Hamkuishi duniani ila muda mchache tu. Na lau ingeli kuwa mnajua malipo ya ukafiri na uasi na kwamba starehe ya duniani ni chache mngeli amini na mkat'ii.

115 Je! Mlidhani kuwa tulikuumbeni bila ya hikima ndio mkafanya ufsadi katika ardhi, na mkadhani kuwa hamtafululiwa mpate kulipwa?

116 Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu peke yake. Na Yeye ndiye Mwenye kumiliki ufalme wote. Hapana

117. Na anaye muomba - pamoja na Mwenyezi Mungu - mungu mwengine hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hisabu yake iko kwa Mola wake Mlezi. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi.¹¹⁷

118. Nawe sema: Mola wangu Mlezi! Samehe na urehemu nawe ni Mbora wa wanao rehemu.¹¹⁸

Mwenye kuabudiwa kwa Haki isipo kuwa Yeye. Na Yeye ndiye Mwenye A'rshi Tukufu.

117 Na mwenye kumuabudu mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu hana ushahidi wa kumfanya huyo astahiki kuabudiwa. Hakika Mwenyezi Mungu atampa adhabu kwa ushirikina wake bila ya shaka yoyote. Hakika makafiri hawaongokewi. Bali watao ongokewa ni Waumini.

118 Na sema, ewe Nabii, ukimlingania Mwenyezi Mungu na kumnyenyekea: Ewe Mola wangu Mlezi! Nisamehe dhambi zangu, na nirehemu. Kwani Wewe ni Mbora wa wanao rehemu, kwa sababu rehema yako imeenea na ipo karibu kwa watendao mema.

Sura 24 - An-Nur

Utangulizi

Sura hii ni ya Madina, na Aya zake ni 64. Mwenyezi Mungu amebainisha ndani yake waajibu wa kusafisha umma na uchafu wa zina na kutangaza fedheha kwa vitendo na maneno kati ya Waumini. Na akaleta sharia ya adhabu kuzuia hayo, kama alivyo leta sharia makhsusi katika uzinzi wa mume au mke ili kujenga imani baina ya mtu na mkewe. Kutoka uzinzi masimulizi yakaingilia kutaja hukumu ya uwongo katika hali hizi, na yawapasayo Waumini kwa min tarafu ya neno ovu lisio kuwa na dalili. Tena yakafuatia masimulizi ya adabu za kuingia majumbani. Na nani mwenye haki ya kuona pambo la mwanamke. Na baada ya wito wa jumla ikafuatiliza kutakiwa mwendo safi usio na towa. Kisha imekuja Nuru ya Mwenyezi Mungu, na inatajwa misikiti, na vinatangazwa vitendo vya makafiri na hali za wenye inadi. Na upande mwingine zinaelezwa hali za Waumini. Baada ya hayo Sura inaeleza adabu za watu wa nyumbani, watu walio khusiana, watoto na wakubwa, katika hali ya kuingiliana na kuchanganyika. Na nani mwenye haki ya kula naye mtu. Na khatimaye zimetajwa sifa za Waumini wanapo itwa na Mtume kwa jambo lilio wakhusu wote, na Sura ikambainisha Mwenye Ukuu wa Ufalme wake ulio tukuka, na Mwenye kuenea ujuzi wake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. HII NI SURA Tuliyo iteremsha na tukailazimisha; tukateremsha ndani yake Aya zilizo wazi ili mkumbuke.¹
2. Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mtandikeni kila mmoja katika wao bakora mia. Wala isikushikeni huruma kwa ajili yao katika hukumu ya Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na lishuhudie adhabu yao kundi la Waumini.²
3. Mwanamume mzinifu hamwoi ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina. Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mshirikina. Na hayo yameharimishwa kwa Waumini.³
4. Na wanao wasingizia wanawake mahashumu, kisha wasilete mashahidi wane, basi

1 Sura hii tumeifunua na tumewajibisha hukumu zake, na tumeteremsha ndani yake dalili zilizo wazi za kuthibitisha uwezo wa Mwenyezi Mungu na upweke wake, na kwamba Kitabu hichi kinatoka kwake, ili mpate kuwaidhika.

2 Na miongoni mwa hukumu hizo ni hukumu ya mwanamke na mwanamume wenye kuzini. Basi kila mmoja wao mpigeni fimbo mia. Wala huruma kwao isikuzieni kutimiza hukumu, ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Kwani yanayo takikana na Imani ni kukhiari kumridhi Mwenyezi Mungu kuliko kuwaridhi watu. Na wahudhurie baadhi ya jamaa Waumini waone hiyo adhabu inavyo tekelezwa, ili adhabu hiyo iwatishie wenginewe wasitende hivyo.

3 Mwanamume muovu aliye zoea uzinifu hapendi kumwoa ila mchafu anaye zini au mshirikina. Na mwanamke mchafu ambaye kazi yake ni uzinifu hapendelei kuolewa ila na mchafu anaye zini; au mshirikina. Na ndoa namna hii haiwaelekei Waumini, kwa kuwa imeshabihiki fiski na kupelekea kutuhumiwa. (Tazama Maelezo 24:3)

watandikeni bakora thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena. Na hao ndio wapotovu.⁴

5. Isipo kuwa wale walio tubu baada ya hayo na wakatengenea; kwani bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mwenye kurehemu.⁵

6. Na wale wanao wasingizia wake zao na hawana mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushuhudia mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba hakika yeye ni katika wasema kweli.⁶

7. Na mara ya tano kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa ni miongoni mwa waongo.⁷

8. Na mke itamwondokea adhabu kwa kutoa shahada mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba huyu mume ni miongoni mwa waongo.⁸

9. Na mara ya tano ya kwamba ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kama mumewe yu miongoni mwa wanao sema kweli.⁹

10. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake, na ya kuwa Mwenyezi Mungu ni Mpokeaji toba.¹⁰

11. Hakika wale walio leta uwongo ni kundi miongoni mwenu. Msifikiri ni shari kwenu, bali hiyo ni kheri kwenu. Kila mtu katika wao atapata aliyo yachuma katika madhambi. Na yule aliyejitwika sehemu yake kubwa miongoni mwao, atapata adhabu kubwa.¹¹

12. Kwa nini mlipo sikia khabari hii, wanaume Waumini na wanawake Waumini hawakuwadhanja wenzao mema, na kusema: Huu ni uzushi dhaahiri?¹²

4 Na wanao watuhumu wanawake wenye hishima zao wasio na makosa kwa tuhuma ya uzinzi bila ya kuleta mashahidi wane wa kuthibitisha tuhuma yao, waadhibuni kwa kuwapiga fimbo thamanini, na wala ushahidi wao usikubaliwe tena kwa jambo lolote muda wa uhai wao. Basi hawa ndio wanao faa kuitwa kwa jina la walio toka vibaya kwenye mipaka ya Dini. (*Tazama Maelezo 24:4*)

5 Lakini mwenye kutubu katika wao akajuta kwa maasi yake, na akaazimia kuwa mt'iifu na kuonyesha ukweli wa toba yake kwa kwenda kwake mwendo mwema, basi Mwenyezi Mungu atamsamehe kumuadhibu.

6 Na hao wanao watuhumu wake zao kuwa wamezini na hawana mashahidi wanao takikana kushuhudia ukweli wa tuhuma yao, basi anatakikana mmoja wa hao kama anataka isimpate adhabu, ashuhudie kwa Mwenyezi Mungu mara nne kuwa yeye ni mkweli katika hiyo tuhuma yake.

7 Na mara ya tano aseme kuwa yeye anastahiki kutengwa na rehema ya Mwenyezi Mungu akiwa ni mwenye kusema uwongo kwa hayo.

8 Baada ya haya mwanamke akinyamaza kimya itampasa kupata adhabu ya uzinzi. Ili kujikinga na adhabu yampasa ashuhudie kwa Mwenyezi Mungu mara nne kwamba mumewe ni mwongo kumtuhumu yeye kwa uzinzi.

9 Na ataje katika mara ya tano kuwa yeye mwanamke anastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu imshukie ikiwa mumewe ni mwenye kusema kweli katika tuhuma yake.

10 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hakukufanyieni fadhila na akakurehemuni, na kuwa Yeye ni Mwingi wa kukubali toba za waja wake, na Mwenye hikima katika vitendo vyake vyote, asingeli kufanyieni sharia za hukumu hizi, na angeli fanya haraka kukuadhibuni duniani kwa maasia.

11 Hakika hao walio zua uwongo ulio potoka na kila uwongofu kumzulia Aisha, mke wa Nabii s.a.w. walipo mtangazia uzushi, ni kikundi wanao ishi pamoja nanyi. Msidhani kituko hichi ni shari kwenu, bali ndiyo kheri yenu; kwa sababu kimewapambanua baina ya wanaafiki na Waumini wa kweli. Na ukadhirihi ukarimu wa walio wema na wenye kuingiwa na uchungu. Na kila mtu katika hawa walio tuhumu watapata malipo yao kwa mujibu wa kadri alivyo shiriki katika uzushi huu. Na mkuu wa kikundi hichi ndiye ataye pata adhabu kubwa kwa ukubwa wa makosa yake.

12 Ilikuwa inavyo takikana kwa Imani ni kuwa wakati wa kusikia huu uzushi, ni Waumini wanaume na wanawake wajidhanie nafsi zao kheri ya usafi na unadhifu, na waseme kwa kupinga: Huu ni uwongo ulio

13. Kwa nini hawakuleta mashahidi wane? Na ilivyo kuwa hawakuleta mashahidi wane basi hao mbele ya Mwenyezi Mungu ni waongo.¹³
14. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake katika dunia na Akhera, bila ya shaka ingeli kupatani adhabu kubwa kwa sababu ya yale mliyo jiingiza.¹⁴
15. Mlipo yapokea kwa ndimi zenu na mkasema kwa vinywa vyenu msiyo yajua, na mlifikiri ni jambo dogo, kumbe mbele ya Mwenyezi Mungu ni kubwa.¹⁵
16. Na kwa nini mlipo yasikia msiseme: Haitufalii kuzungumza haya. Subhanak Umetakasika! Huu ni uzushi mkubwa!¹⁶
17. Mwenyezi Mungu anakuonyeni msirejee tena kufanya kama haya kabisa, ikiwa nyinyi ni Waumini!¹⁷
18. Na Mwenyezi Mungu anakubainisheni Aya. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.¹⁸
19. Kwa hakika wale wanao penda uenee uchafu kwa walio amini, watapata adhabu chungu katika dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui.¹⁹
20. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake, na kuwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole, Mwenye kurehemu.²⁰
21. Enyi mlio amini! Msizifuate nyayo za Shet'ani. Na atakaye fuata nyayo za Shet'ani basi yeye huamrisha machafu na maovu. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema yake juu yenu, asingeli takasika miongoni mwenu kabisa hata mmoja. Lakini Mwenyezi Mungu humtakasa amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.²¹

wazi umezuliwa, kwa kuwa haya yamemkhusu bora ya Mitume na bora ya wanawake walio wa kweli.

13 Je! Hao wazushi walileta mashahidi wane wa kushuhudia hayo waliyo yasema? Hawakufanya hayo... Na ikiwa hawakufanya basi hao kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu ni waongo.

14 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hakukufanyieni fadhila kwa kubainisha hukumu, na hakukurehemuni duniani kwa kuacha kuleta adhabu kwa haraka, na Akhera kwa kukusameheni, angeli kuteremshieni adhabu kubwa kwa sababu ya kujiingiza kwenu katika uzushi huu.

15 Mmezichukua khabari hizo kwa ndimi zenu na mkazieneza kati yenu. Wala nyinyi hamkujua kuwa hizo ni khabari za kweli, na mkaona jambo hili ni dogo si la kuadhibiwa na Mwenyezi Mungu, au sana adhabu yake ni ndogo; na ilhali ni jambo kubwa kweli la kuadhibiwa adhabu kali na Mwenyezi Mungu.

16 Yanayo faa ni kuwa baada ya kusikia maneno haya ya uwongo ni kuambizana msiyazungumze, kwa sababu si laiki yenu, na mustaajabie kuzuliwa uwongo muovu wa namna hii wa khatari.

17 Na hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni msirudie tena kufanya maasi namna hii kabisa, ikiwa nyinyi ni Waumini wa kweli. Kwani sifa za Imani zinapingana na mwendo huu.

18 Na Mwenyezi Mungu anakuteremshieni Aya zenye kuonyesha hukumu kwa uwazi dhaahiri. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa Ujuzi, hapana asicho kijua katika vitendo vyenu. Naye ni Mwenye hikima kwa kila anacho kitungia sharia na kukiumba. Kwani kila sharia zake na uumbaji wake ni kwa mujibu wa hikima.

19 Hakika hao wanao penda kutangaza machafu, wakayatangaza baina ya Waumini watapata adhabu yenye kutia uchungu duniani kwa mateso yaliyo kwisha pasishwa, na Akhera watatiwa Motoni ikiwa hawato tubu. Na Mwenyezi Mungu anajijua vyema hali zenu zote, za dhaahiri na zilizo fichikana. Na nyinyi hamjui anayo yajua Yeye.

20 Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake kwenu, na kuwa Yeye ni Mwingi wa upole, Mkunjufu wa rehema, asingeli kubainishieni hukumu, na angeli kuleteeni mateso kwa haraka hapa duniani kwa maasi yenu.

21 Enyi mlio amini! Hifadhini nafsi zenu kwa Imani. Wala msimfuate Shetani anaye kuvutieni kwenda tangaza uchafu na maasi baina yenu. Na mwenye kumfuata Shetani basi huyo amekwisha a'si, kwani Shetani anaamrisha madhambi makubwa makubwa na maasi mabaya. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi

- 22.** Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wasaa wasiape kutowapa jamaa zao na masikini na walio hama kwa Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.²²
- 23.** Hakika wanao wasingizia wanawake, wanao jihishimu, walio ghafilika, Waumini, wamelaaniwa duniani na Akhera, nao watapata adhabu kubwa.²³
- 24.** Siku ambayo zitawashuhudia ndimi zao na mikono yao na miguu yao kwa waliyo kuwa wakiyatenda.²⁴
- 25.** Siku hiyo Mwenyezi Mungu atawapa sawa sawa malipo yao ya haki, na watajua kwamba hakika Mwenyezi Mungu ndiye Haki Iliyo Wazi.²⁵
- 26.** Wanawake waovu ni wa wanaume waovu, na wanaume waovu ni wa wanawake waovu. Na wanawake wema ni wa wanaume wema, na wanaume wema ni wa wanawake wema. Hao wameepushwa na hayo wanayo yasema; wao watapata msamaha na riziki ya ukarimu.²⁶
- 27.** Enyi mlio amini! Msiingie nyumba zisio nyumba zenu mpaka mwombe ruhusa, na mwatolee salamu wenyewe. Hayo ni bora kwenu mpate kukumbuka.²⁷
- 28.** Na msipo mkuta mtu humo basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkiambiwa: Rudini! Basi rudini. Hivi ni usafi zaidi kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayo yatenda.²⁸

Mungu juu yenu na rehema yake kwenu kwa kubainisha hukumu na kukubali toba ya wenye kuasi asinget'ahirika hata mmoja wenu na uchafu wa maasi. Lakini Mwenyezi Mungu anamsafisha mwenye kumuelekea Yeye kwa kumwezesha kuwa mbali na maasi, au kwa kumsamehe kwa kutubu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia kila kauli, Mwenye kujua kila kitu, na atakulipeni kwayo.

22 Wala wasiape wema wenu wenye nafasi kuwa watazuia kuwafanyia hisani jamaa zao na masikini na walio hama makwao katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wengineo kwa sababu za kibinafsi, kama vile kuwa wamewatendea uovu fulani. Lakini inatajikana wawasamehe na wayaachilie mbali makosa yao. Na ikiwa mnapenda Mwenyezi Mungu akusameheni maovu yenu basi wafanyieni wanao kufanyieni mabaya mfano wa anavyo kufanyieni nyinyi Mola wenu Mlezi. Na fuateni mwendo wake kwani Yeye ni Mkunjufu wa kusamehe na kurehemu. (*Tazama* Maelezo 24:22)

23 Hakika hao wanao wasingizia wanawake wema walio safi, ambao hawadhaniwi hayo, bali wao kwa kumshughulikia Mwenyezi Mungu hata wameghafilika na hayo wanayo singiziwa, Mwenyezi Mungu atawatenga mbali na rehema yake katika dunia na Akhera, na watapata adhabu kubwa ikiwa hawatotubu.

24 Adhabu hiyo itakuwa Siku ya Kiyama ambapo itakuwa hapana njia za kuikataa. Bali waliyo yatenda yatathibiti juu yao, kwa kuwa zitawashuhudia ndimi zao, na mikono yao, na miguu yao, kwa madhambi yote waliyo yatenda. Na hayo ni kwa kudhihiri athari ya vitendo vyao juu ya viungo hivyo, au kwa kutamkisha na Mwenyezi Mungu ambaye anatamkisha kila kitu.

25 Siku hiyo Mwenyezi Mungu atawaadhibu adhabu iliyo kwisha hukumiwa wapewe kwa ukamilifu wake bila ya upungufu. Na hapo wataujua kwa ujuzi wa yakini Ungu wa Mwenyezi Mungu na hukumu za Sharia yake, na ukweli wa ahadi yake na kitisho chake. Kwani yote hayo yatakuwa wazi hayana kificho.

26 Wanawake waovu ni wa wanaume waovu, na wanaume waovu ni wa wanawake waovu. Na kadhaalika wanawake wema ni wa wanaume wema, na wanaume wema ni wa wanawake wema. Basi yamkini vipi kuwepo uwovu katika wema ulio hifadhiwa, nao ni mke wa mwema muaminifu Mtume Mtukufu s.a.w.? Na wema hawa wamehifadhika na tuma wanazo wasingizia hao waovu. Na wao wana maghfira ya Mwenyezi Mungu kwa vijidhambi vidogo vidogo ambavyo mwanaadamu hakosekani kuwa navyo. Na watapata ukarimu mkubwa wa kupata neema za Peponi.

27 Enyi mlio amini! Msiingie katika nyumba zisio kuwa zenu ila baada ya kutaka idhini kwa wakaazi wake na mkaruhusiwa kuingia, na baada ya kuwatolea salamu wakaazi wake - na salamu ni bora kwenu kuliko kuingia tu bila ya kutoa salamu. Na Mwenyezi Mungu amekuwekeeni sharia hii ili mpate kunasihika na muifuate.

28 Na ikiwa katika hizo nyumba hamkumkuta mtu wa kukupeni idhini basi msiingie mpaka aje wa

29. Si vibaya kwenu kuingia nyumba zisio kaliwa ambazo ndani yake yamo manufaa yenu. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayo yadhahirisha na mnayo yaficha.²⁹

30. Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za wanayo yafanya.³⁰

31. Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao isipo kuwa unao dhahirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasionyeshe uzuri wao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenzao, au iliyo wamiliki mikono yao ya kuume, au wafwasi wanaume wasio na matamania, au watoto ambao hawajajua mambo yaliyo khusu uke. Wala wasipige chini miguu yao ili yajuulikane mapambo waliyo yaficha. Na tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waumini, ili mpate kufanikiwa.³¹

32. Na waozeni wajane miongoni mwenu na wema katika watumwa wenu na wajakazi wenu. Wakiwa mafakiri Mwenyezi Mungu atawatajirisha kwa fadhila yake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa Mwenye kujua.³²

33. Na wajizuilie na machafu wale wasio pata cha kuolea, mpaka Mwenyezi Mungu awatajirisha kwa fadhila yake. Na wanao taka kuandikiwa uhuru katika wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki, basi waandikieni kama mkiona wema kwao. Na

kukuruhusuni. Na ikiwa hakukuruhusuni na akakutakeni mrudi nyuma, basi rudini; wala msishikilie kutaka ruhusa ya kuingia. Kwani kurejea nyuma ni hishima zaidi na usafi zaidi kwa nafsi zenu. Na Mwenyezi Mungu anajua vyema hali zenu zote na atakulipeni, basi msende kinyume na uwongozi wake.

29 Na mkitaka kuingia nyumba za umma zisio kaliwa na watu makhsusi na ndani yake zipo haja zenu, kama vile maduka, mahoteli, nyumba za ibada, hapana ubaya kuingia bila ya kutaka ruhusa. Na Mwenyezi Mungu anajua kwa ujuzi wa timamu kabisa vitendo vyenu vyote vya dhaahiri na vilivyo fichikana. Basi tahadharini na kwenda kinyume naye.

30 Ewe Nabii! Waambie Waumini katika yanayo pelekea zina na kutilisha shaka, wasitazame yanayo harimishwa kutazama, nayo ni tupu za wanawake na sehemu za uzuri wao, na wanaume wahifadhi tupu zao kwa kuzisitiri na kuto zitumilia kwa njia isiyo ruhusiwa na Sharia. Adabu hiyo ndio ina hishima zaidi na safi zaidi kwao wasiingie katika maasi na tuhuma. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua baraabara yote wayatendayo, na atakuja walipa kwao.

31 Vile vile ewe Nabii, waambie wanawake Waumini, wanaamrisha waache kutazama yaliyo harimishwa, na wazihifadhi tupu zao kwa kuzisitiri na kutoingiliwa ila kwa njia ya Kisharia. Na wasiwaonyeshe wanaume ya kuwavutia katika uzuri wa umbo lao na mapambo, kama kifua, mabega, vidani, isipo kuwa yale tangu hapo yamedhihiri, kama uso na mikono. Na ewe Nabii! Watake hao wanawake wajisitiri mwahali zilipo funuka nguo, kama shingo na kifua. Na hayo kwa kuteremshia vitambaa vya kichwani. Na wasiachilie kuonekana uzuri wao ila kwa waume zao, na jamaa ambao ni haramu kuoana nao milele, kama baba zao, au baba za waume wao, au watoto wao, au watoto wa waume zao kwa wake wengine, au kaka zao, au watoto wa kaka zao, au watoto wa dada zao. Na mfano wa hawa ni wanawake wenzao, sawa sawa wakiwa waungwana au wajakazi, na wanaume wanao ishi nao na hawana tena haja ya wanawake kwa ukongwe. Na kadhaalika watoto wadogo ambao hawajafikilia miaka ya kutamani. Na pia watake wanawake wasifanye vituko vya kutaka kuwavutia wanaume kama kugonga miguu chini ili isikilizane milio ya mitali na kugesu iliyo fichikana ndani ya nguo. Na tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waumini, kwa mlivyo iacha amri ya Mwenyezi Mungu. Na shikamaneni na adabu za Dini mpate kuongokewa katika dunia na Akhera yenu

32 Na saidieni katika kujitenga na zina na yanayo pelekea zina, kwa kuwaoza ambao bado hawajaoana miongoni mwa wanaume wenu na wanawake wenu, na walio kuwa wanafaa kwa hayo katika watumwa wenu. Na wala umasikini usiwe sababu ya kuzuilia kuoa. Kwani Mwenyezi Mungu atasahilisha njia za maisha mazuri kwa mwenye kutaka kuishi maisha safi. Na fadhila za Mwenyezi Mungu ni kunjufu, na Yeye anajua kabisa niya za watu, na kila lipitalo katika ulimwengu.

wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu aliyo kupeni. Wala msiwashurutishe vijakazi vyenu kufanya zina kwa ajili ya kutafuta pato la maisha ya dunia, ilhali wao wanataka kujihishimu. Na atakaye walazimisha basi Mwenyezi Mungu baada ya kulazimishwa kwao huko, atawasamehe, kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.³³

34. Na kwa yakini tumekuteremshieni Ishara zilizo wazi na mifano kutokana na walio tangulia kabla yenu na mawaidha kwa wachamngu.³⁴

35. Mwenyezi Mungu ni Nuru ya Mbingu na Ardhi. Mfano wa Nuru yake ni kama shubaka lenye kuwekwa ndani yake taa. Taa ile imo katika tungi. Tungi lile ni kama nyota inayo meremeta, inayo washwa kwa mafuta yanayo toka katika mti ulio barikiwa, mzaituni. Si wa mashariki wala magharibi. Yanakaribia mafuta yake kung'aa wenyewe ingawa moto haujayagusa - Nuru juu ya Nuru. Mwenyezi Mungu humwongoa kwenye Nuru yake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.³⁵

36. Katika Nyumba ambazo Mwenyezi Mungu ameamrisha zitukuzwe, na humo

33 Na ambao hawakupata uwezo wa fedha za kuolea basi wafuate mojawo wa njia nyengine kama saumu na riyadha na kazi za kutumia akili. Kwa hayo hujikurupusha mpaka Mwenyezi Mungu akawafungulia kwa fadhila zake zitakazo wawezesha kuoa. Na watumwa ambao wanataka kuandikiana nanyi ili wapate uhuru wao ni waajibu juu yenu kuwakubalia walitakalo, mkijua kuwa watatimiza kutekeleza na wanaweza. Na juu yenu kuwasaidia waweze kutimiza walio andikiana nanyi, na hayo ama ni kwa kuwapunguzia shuruti mlizo andikiana nao, au kwa kuwapa mali katika mali aliyo kuneemesheni Mwenyezi Mungu, mkawapa katika Zaka au Sadaka. Na ni haramu juu yenu kuwafanya vijakazi vyenu njia ya pato la duniani rakhisi kwa kuwafanya makahaba, na mkawalazimisha kwa hayo. Na vipi mnakwenda kumlazimisha uchafu anaye taka kuwa safi? Na mwenye kuwalazimisha, basi Mwenyezi Mungu humsamehe mwenye kulazimisha pindi akitubu kwa dhambi zake za kulazimisha. Kwani hakika Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa maghfira na rehema. (*Tazama Maelezo 24:33*)

34 Na Sisi tumekuteremshieni katika Sura hii na nyenginezo Aya zilizo wazi zenye kubainisha hukumu. Na tumekuteremshieni mifano ya hali mbali mbali za walio tangulia, na uwongozi, na mawaidha ambayo kwayo watapata faida wenye kumkhofu Mwenyezi Mungu.

35 Mwenyezi Mungu ndiye chanzo cha Nuru ya katika mbingu na ardhi. Yeye ndiye Mwenye kunawirisha vyote hivyo kwa nuru yote tunayo iona na tukenda ndani yake, na ya maana, kama Nuru ya Haki na uadilifu, na ilimu, na fadhila, na uwongofo, na Imani, na kwa ushahidi na athari kama alivyo waahidi viumbe vyake, na kwa vyote vinavyo onyesha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, na vikalingania Imani kumuamini Yeye *Subhanahu*. Na mfano wa Nuru yake Tukufu na dalili zake zilizo zagaa kwa uwazi ni kama mfano wa Nuru ya taa yenye kung'aa kwa ukali kabisa, iliyo wekwa kwenye shubaka la ukutani ili kuukusanya mwangaza wake na kuzidi kuupa nguvu. Na taa hiyo imevikwa tungi la kigae safi linameremeta kama inavyo meremeta nyota. Na taa ile inawaka kwa mafuta ya mti wenye baraka nyingi, ulio pandwa kwenye udongo mzuri na pahali pazuri. Mti huu ni mzaituni unao mea pahala pa kati na kati. Basi huo si wa mashariki ukakosa joto la jua wakati wa alasiri, wala si wa magharibi ukakosa joto la jua wakati wa asubuhi. Bali huo uko juu ya kilele cha mlima, au katika uwazi wa ardhi unao patisha jua mchana kutwa. Mafuta ya mti huu yanakaribia kutoa mwanga kwa ubora wa usafi wake hata ikiwa hayajaguswa na moto wa taa. Mambo haya yote yanazidisha mwangaza wa hiyo taa juu ya mwangaza wake, na Nuru juu ya Nuru.

Na namna hii ndio zinakuwa dalili zilizo enea katika ulimwengu, za kuonekana na kupimika kwa akili; ni Ishara zilizo wazi hazitaki kutiliwa shaka yoyote kwa kuwepo Mwenyezi Mungu, na kuwajibikia Imani kumuamini Yeye, na Risala za Mitume aliyo waleta. Na Mwenyezi Mungu humwezesha kufikia Imani amtakaye kwa njia ya dalili hizi ikiwa huyo mtu atajaribu kunafika na nuru ya akili yake. Na Mwenyezi Mungu ameleta mifano ya kuweza kuhisiwa na kuonekana ili iwe wepesi kuelewa mambo ya kiakili. Na Yeye *Subhanahu* ni Mkunjufu wa ujuzi, anawajua wenye kuangalia Ishara zake na wenye kuzipuza na wakapanda kiburi. Naye atawalipa kwa hayo.

litajwe jina lake, wanamtakasa humo asubuhi na jioni.³⁶

37. Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kushika Sala, na kutoa Zaka. Wanaikhofu Siku ambayo nyoyo na macho yatageuka.³⁷

38. Ili Mwenyezi Mungu awalipe bora ya waliyo yatenda, na awazidishie katika fadhila zake. Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.³⁸

39. Na walio kufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji. Hata akiyaendea hapati chochote. Na atamkuta Mwenyezi Mungu hapo naye amlipe hisabu yake sawa sawa. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.³⁹

40. Au ni kama giza katika bahari kuu, iliyo funikwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu. Giza juu ya giza. Akiutoa mtu mkono wake anakaribia asiune. Na ambaye Mwenyezi Mungu hakumjaalia kuwa na nuru hawi na nuru.⁴⁰

41. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu vinamtakasa vilivyomo katika mbingu na ardhi, na ndege wakijua mbawa zao? Kila mmoja amekwisha jua Sala yake na namna ya kumtakasa kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua wayatendayo.⁴¹

36 Hakika wapo watu wanao mtakasa Mwenyezi Mungu na wanamuabudu misikitini ambayo Mwenyezi Mungu ameamrisha ijengwe na iamirishwe kwa kudhukuriwa Mwenyezi Mungu, nao wameshughulikia hayo asubuhi na jioni.

37 Dunia na yaliomo duniani ya kuuza na kununua hayawashughulishi wakaacha kumdhukuru Mwenyezi Mungu na kumzingatia. Wao wanashika Sala, na wanatoa Zaka, na huku wakiikhofu Siku ya Kiyama ambapo nyoyo zitakuwa hazina utulivu kwa sababu ya wasiwasi na hamu, na kungojea matokeo, na macho yatadahadari kwa mhangaiko na kushtuka kwa vituko vigeni wanavyo viona, na wingi wa vitisho.

38 Na malipo ya vitendo vyao ni kulipwa sawa sawa kwa ubora wa malipo kwa vitendo vyao vyema, na watapata fadhila kwa kupewa zaidi kuliko wanavyo stahiki. Kwani Yeye *Subhanahu* ni Mkunjufu wa fadhila, humpa amtakaye katika waja wake wema kipao kikubwa, asichoweza mtu kukihisabu wala wenye kuhisabu hawawezi kukisia.

39 Na hao walio pinga na wakakanya wanadhani wenyewe kuwa wamefanya vizuri, na kwamba vitendo vyao vizuri vitawaletea faida Siku ya Kiyama. Lakini hao wamekosea katika dhana yao hiyo. Kwani mfano wa vitendo vyao katika upotovu wake na kukosa maana ni kama mmetuko unao tokea unapo angukia mwako wa jua wakati wa aduhuri juu ya ardhi tambarare jangwani. Mwenye kiu hudhania kuwa ni maji. Hata akiyafikia asikute chochote chenye manufaa kama alivyo dhania. Hali kadhaalika vitendo vya makafiri siku ya malipo vitakuwa vumbi lilio tawanyika. Na kafiri ataikuta adhabu ya Mwenyezi Mungu inamngojea kwa utimilivu wake bila ya nuksani. Hakika hisabu ya Mwenyezi Mungu hapana shaka inakuja. Na Yeye, Aliye takasika, ni Mwepesi katika kuhisabu kwake, hachelewi wala hakosei.

40 Na huu mfano mwengine wa vitendo vya makafiri. Mfano wake ni mfano wa giza la bahari kubwa iliyo tanda yenye kina kirefu. Mawimbi yake yanapigana na kusukumana wenyewe kwa wenyewe. Nayo yamefunikwa na mawingu mazito meusi hayapitishi mwangaza. Katika giza hili lililo rundikana msafiri wa baharini awezi kuuona mkono wake hata akiukurubisha machoni. Basi anabaki ameduwaa amebabaika hajijui. Na vipi ataona kitu atokane na butaa hili bila ya kupata Nuru ya kumwongoa katika mwendo wake, na kumwoko na kugongana na kuhiliki. Na basi kama hali hiyo hiyo makafiri hawapati faida katika vitendo vyao, wala hawatoki katika upofu wao na upotovu wao, wala hawajiokoi nafsi zao, ila kwa Nuru ya Imani. Kwani hana Nuru ya kumwongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka. Basi atakuwa katika walio teketea. (*Tazama Maelezo 24:40*)

41 Ewe Nabii! Hujui kwa yakini kwamba kwa Mwenyezi Mungu hunyenyekea kila kiliomo mbinguni na duniani? Na wanamnyenyekea ndege vile vile, nao wamekunjua mbawa zao? Basi viumbe vyote hivi vinanyenyekea amri ya Mwenyezi Mungu na mipango yake. Vinamtakasa na washirika na kila lisio na laiki naye. Na kila kimojawapo kinajua kwa kujaaliwa na Mwenyezi Mungu yaliyo kiwajibikia katika unyenyekevu na kutakasa na kutimiza wadhifa wa maisha. Na Mwenyezi Mungu nyuma yao anajua kwa utimilivu wa kujua Sala ya kila mwenye kusali, na kusabihi kwa mwenye kusabihi, na yote wayafanyayo

42. Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na ardhi, na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya wote.⁴²
43. Je! Huoni ya kwamba Mwenyezi Mungu huyasukuma mawingu, kisha huyaambatisha, kisha huyafanya mirundi? Basi utaona mvua ikitoka kati yake. Na huteremsha kutoka juu kwenye milima ya mawingu mvua ya mawe, akamsibu nayo amtakaye na akamuepusha nayo amtakaye. Hukurubia mmetuko wa umeme wake kupofua macho.⁴³
44. Mwenyezi Mungu hubadilisha usiku na mchana. Hakika katika hayo yapo mazingatio kwa wenye kuona.⁴⁴
45. Na Mwenyezi Mungu ameumba kila kinyama kutokana na maji. Wengine katika wao huenda kwa matumbo yao, na wengine huenda kwa miguu miwili, na wengine huenda kwa miguu mine. Mwenyezi Mungu huumba ayatakayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.⁴⁵
46. Kwa yakini tumeteremsha Ishara zinazo bainisha. Na Mwenyezi Mungu hummwongoa amtakaye kwenye Njia Iliyo Nyooka.⁴⁶
47. Na wanasema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume, na tumet'ii. Kisha kikundi katika hao hugeuka baada ya hayo. Wala hao si wenye kuamini.⁴⁷
48. Na wanapo itwa kumuendea Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu baina yao, kipo kikundi katika wao kinakataa.⁴⁸

waja. Basi huwaje makafiri wakawa hawaamini?

42 Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kumiliki mbingu na ardhi na viliomo ndani yao, na ndiye Mwenye madaraka juu yao, na wote watarejea kwake Siku ya Kiyama kwa ajili ya hisabu na malipo.

43 Ewe Nabii! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu huyavuta mawingu, kisha huyakusanya na kuyarindika moja juu ya moja. Utaona mvua inatoka kwenye mawingu. Na Mwenyezi Mungu huteremsha kutokana na mawingu yaliyo rindikana yanayo shabihi milima kwa ukubwa wake, vipande vya barafu kama changarawe, vikawaangukia watu vikawaletae manufaa au madhara, kufuatana na kanuni zake na matakwa yake, wala asiwateremshie wenginewe kwa mujibu apendavyo Yeye *Subhanahu*, Mtendaji, Mwenye kukhitari. Mwangaza wa umeme unao tokea kwa kugongana mawingu hukaribia kutia upofu kwa ukali wake. Na mambo kama haya ya kuonekana ni dalili za kuonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu ambao unao wajibisha kuleta Imani ya kumuamini Yeye. (*Tazama Maelezo 24:43*)

44 Mwenyezi Mungu huzigeuza hali za usiku na mchana kwa urefu na ufupi, na kwa kuanzia na kumalizikia, kwa mizunguko ya falaki. Hakika katika hayo pana mazingatio kwa wenye akili zilizo nzima zenye busara, na kwa njia hiyo wakamuamini Mwenyezi Mungu.

45 Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu. Na ndiye aliye anzisha kila kitu kwa kupenda kwake. Na akaumba kila kilicho hai kutokana na asili moja ya shirika, nayo ni maji. Na kwa hivyo kila kihai hakiachi kuwa na maji. Kisha zinawakhitalifisha khitilafu nyengine kwa namna, na uwezo, na sura, na kadhaalika. Katika wanyama wapo wanao tambaa kwa matumbo yao, kama samaki, na nyoka. Na wapo wanao kwenda kwa miguu miwili kama wanaadamu na ndege. Na wapo wanao kwenda kwa miguu mine kama mahayawani wengi wa kufugwa na wa mwituni. Mwenyezi Mungu huumba apendavyo kwa njia mbali mbali, kuonyesha uwezo wake na ujuzi wake. Kwani ni Mwenye kutaka atakacho, na Mwenye kukhitari apendacho. Na Yeye ni Muweza wa kila kitu. (*Tazama Maelezo 24:45*)

46 Na hakika Sisi tumeteremsha kwa wahyi Aya zilizo wazi za kubainisha hukumu na mawaidha, na zinazo piga mifano. Na Mwenyezi Mungu humwezesha kwenye kheri ampendaye katika waja wake ambao wapo tayari kuziangalia na kufaidika nazo.

47 Na wanaafiki husema kwa ndimi zao: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume, na tunazifuata amri zao. Na wanapo tiwa mtihanini kikundi kati yao hukataa kushirikiana na Waislamu katika kazi ya kheri, kama Jihadi na nyenginezo, baada ya kauli yao hii. Na watu hawa si Waumini wa kweli, wala hawastahiki kutumiliwa jina la Waumini kwao.

48 Na katika hali zao ni kuwa wakitakiwa kuhukumiwa mbele ya Mtume kwa jambo alilo literemsha

49. Na ikiwa haki ni yao, wanamjia kwa kut'ii.⁴⁹

50. Je! Wana maradhi katika nyoyo zao, au wanaona shaka, au wanaogopa ya kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake watawadhulumu? Bali hao ndio madhaalimu.⁵⁰

51. Haiwi kauli ya Waumini wanapo itwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu baina yao, ila ni kusema: Tumesikia, na tumet'ii! Na hao ndio wenye kufanikiwa.⁵¹

52. Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakamwogopa Mwenyezi Mungu na wakamcha, basi hao ndio wenye kufuzu.⁵²

53. Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa kiapo chao ya kwamba ukiwaamrisha kwa yakini watatoka. Sema: Msiapie! Ut'iifu unajuulikana. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.⁵³

54. Sema: Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume. Na mkigeuka, basi yaliyo juu yake ni aliyo bebishwa, na yaliyo juu yenu ni mliyo bebishwa nyinyi. Na mkimt'ii yeye mtaongoka. Na hapana juu ya Mtume ila kufikisha Ujumbe wazi wazi.⁵⁴

55. Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.⁵⁵

Mwenyezi Mungu, unaafiki wa baadhi yao hudhuhiri, na wao hukataa kuhukumiwa wakijua kuwa haki ni ya wale makhasimu zao.

49 Ama wakijua kuwa haki iko upande wao basi humjia Mtume mbio mbio ili awahukumu baina yao na makhasimu zao.

50 Na kwa nini wanasimama msimamo huu katika kushitakiana mbele ya Mtume? Ni kwa sababu nafsi zao zimesibiwa na maradhi ya upofu, na kwa hivyo haziridhiki na hukumu yako ya haki? Au ni kwa kuwa wao wanatilia shaka uadilifu wa Muhammad s.a.w. katika kuhukumu? Si lolote katika hayo kabisa. Lakini hao ni madhaalimu walio dhulumu nafsi zao na wengineo kwa sababu ya ukafiri wao na unaafiki wao na kuiacha kwao haki.

51 Hakika kauli ya haki ifaayo kwa Waumini wa kweli wanapo itwa wahukumiwe kwa mujibu wa yaliyo kuja kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ni kuwa waseme kwa kukubali na kunyenyekea: Tumesikia wito wako, ewe Muhammad! Na tumeridhia hukumu yako. Na hao ndio watao kuwa watu wa kufanikiwa katika dunia yao na Akhera yao.

52 Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na kuridhia anayo yaamrisha Mtume s.a.w. na wakaiogopa dhati ya Mwenyezi Mungu Tukufu, na wakaukumbuka Utukufu wake, na wakaikhofu ghadhabu yake, hao ndio watakao pata radhi ya Mwenyezi Mungu na mapenzi yake, na neema za Pepo, na ndio wenye kupata kheri tupu.

53 Na wanaafiki wanaapa kwa ukomo wa nguvu za viapo vyao, kwamba wewe, Muhammad, ukiwaamrisha watoke nawe kwenda vitani watakut'ii. Waambie: Msiapie! Kwani mambo yatakikanayo kwenu mnayajua, hapana hata mmoja wenu asiye yajua. Wala yamini zenu za uwongo haziondoi ujuzi huo. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua baraabara kila linalo tokana nanyi, na Yeye atakulipeni kwayo.

54 Waambie: Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume kwa ut'iifu wa kweli wenye kuonyesha vitendo vyenu. Wanaafiki wakipuuzwa wasifuata, basi juu ya Muhammad ni waajibu wa aliyo twishwa tu na Mwenyezi Mungu, nayo ni amri ya kufikilisha Ujumbe, wala hakukalifishwa uwongofu wao. Na nyinyi juu yenu ni hayo aliyo kutwikeni Mwenyezi Mungu nayo ni kufuata na kut'ii. Na mtapata adhabu ikiwa mtaendelea na uasi. Na mkimt'ii Mtume mtaongoka kwenye kheri. Na yeye haimpasi ila kufikisha kwa uwazi - mkit'ii au mkiasi - na yeye keshwa fikisha.

55 Mwenyezi Mungu amewaahidi katika nyinyi walio isadiki Haki na wakaifuata, na wakatenda vitendo vyema, kwa ahadi ya kutia mkazo, ya kwamba atawafanya makhalifa (wafwatizi, warithi) wa wale walio watangulia wawarithi katika kuhukumu na utawala katika nchi, kama ilivyo kuwa hali ya walio watangulia. Na atawasimamishia Uislamu kuwa ndio Dini yao aliyo wapendekzee. Basi watakuwa na

56. Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt'iini Mtume, ili mpate kurehemewa.⁵⁶
57. Msiwadhanie walio kufuru kwamba watashinda katika nchi. Na makaazi yao ni Motoni, na hakika ni maovu kweli marejeo yao.⁵⁷
58. Enyi mlio amini! Nawakutakeni idhini iliyo wamiliki mikono yenu ya kulia na walio bado kubaalighi miongoni mwenu mara tatu - kabla ya Sala ya alfajiri, na wakati mnapo vua nguo zenu adhuhuri, na baada ya Sala ya isha. Hizi ni nyakati tatu za faragha kwenu. Si vibaya kwenu wala kwao baada ya nyakati hizi, kuzungukiana nyinyi kwa nyinyi. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo kuelezeni Aya zake, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.⁵⁸
59. Na watoto wanapo fikilia umri wa kubaalighi basi nawatake ruhusa, kama walivyo taka ruhusa wa kabla yao. Hivyo ndivyo anavyo kubainishieni Mwenyezi Mungu Aya zake, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.⁵⁹
60. Na wanawake wazee wasio taraji kuolewa, si vibaya kwao kupunguza nguo zao, bila ya kujishaua kwa mapambo. Na wakijihishimu ni bora kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.⁶⁰
61. Si vibaya kwa kipofu, wala si vibaya kwa kiguru, wala si vibaya kwa mgonjwa, wala kwenu nyinyi, mkila katika nyumba zenu, au nyumba za baba zenu, au nyumba za mama zenu, au nyumba za kaka zenu, au nyumba za dada zenu, au nyumba za ami zenu, au nyumba za shangazi zenu, au nyumba za wajomba zenu, au nyumba za dada wa mama zenu, au za mlio washikia funguo zao, au rafiki yenu. Si vibaya kwenu mkila pamoja au mbali mbali. Na mkiingia katika nyumba, toleaneni salamu, kuwa ni

heba na madaraka. Na ataibadilisha hali yao ya khofu iwe ya amani, wawe wananiabudu Mimi nao wametua. Hawanishirikishi Mimi na chochote kile katika ibada. Na wenye kukhiari ukafiri baada ya ahadi hii ya kweli, au wakartadi wakaacha Uislamu, basi hao ndio walio toka nje, walio asi, wapinzani.

56 Na shikeni Sala kwa ukamilifu wa nguzo katika utulivu na unyenyekevu, ili ipate kuwa inazuia uchafu na mambo mabaya. Na wapeni Zaka wanao stahiki. Na mt'iini Mtume kwa yote anayo kuamrisheni, ili mpate kutaraji rehema ya Mwenyezi Mungu na radhi yake.

57 Ewe Nabii! Usidhani kuwa makafiri wataweza kumkwepa Mwenyezi Mungu asiwashike kwa madhambi yao, au watu wa Haki wasiwaone pahala popote pale katika ardhi. Bali Yeye ni Muweza, na marejeo yao Siku ya Kiyama ni Motoni. Na marejeo maovu kabisa ni marejeo yao.

58 Enyi mlio amini! Yakupaseni muamrishe watumishi wenu na vijana wenu ambao bado hawajabalighi wasikuilingieni vyumbani mwenu ila baada ya kutaka idhini katika nyakati tatu, nazo ni kabla ya Sala ya alfajiri, na pale mnapo punguza nguo zenu wakati wa kupumzika mchana, na baada ya Sala ya Isha mnapo jitayarisha kulala. Kwani nyakati hizi mtu hubadilisha mavazi ya kulalia badala ya mavazi ya kutokea, na huonekana sehemu za mwili ambazo hazifai kuonekana. Wala hapana ubaya kwenu wala kwao kuingia bila ya ruhusa nyakati nyenginezo, kwa sababu ni jambo la ada watu wa nyumbani kupitia kwa maslaha yao. Na kwa uwazi wa namna hii Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya za Qur'ani ili akuwekeeni wazi hukumu. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni Mkunjufu wa ujuzi, Mkubwa wa hikima, anajua yanayo silihi kwa waja wake, na anawatungia Sharia zinazo wanasibu, na kwa kadri ya haja yao. (Tazama Maelezo 24:58)

59 Na vijana vyenu wakifikilia umri wa kubalighi inawapasa watake ruhusa ya kuingia kila nyumba, na kila wakati, kama ilivyo wapasa wenzao wa kabla yao. Na kwa mfano wa uwazi kama huu Mwenyezi Mungu anakuwekeeni wazi Aya zake alizo ziteremsha. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni Mkunjufu wa ujuzi, Mkubwa wa hikima. Anajua linalo wasilishi waja wake, na anawatungia Sharia zinazo wanasibu, na kwa kadri ya haja yao.

60 Na wanawake wakongwe ambao hawatamai kuolewa, hawalaumiwi wakipunguza baadhi ya nguo zao, kwa sharti wasiwe wanajishauwa kwa kuonyesha uzuri wa mwili wao ambao Mwenyezi Mungu ameamrisha usitiriwe. Lakini kujihishimu kwa kujisitiri kwa ukamilifu ni bora kwao kuliko kujifunua. Na Mwenyezi Mungu anawasikia wayasemayo, na anayajua makusudio yao, na atawalipa kwa hayo.

maamkio yanayo toka kwa Mwenyezi Mungu, yenye baraka na mema. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo kubainishieni Aya zake mpate kuelewa.⁶¹

62. Hakika Waumini wa kweli ni walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na wanapo kuwa pamoja naye kwa jambo la kuwakhusu wote hawaondoki mpaka wamtake ruhusa. Kwa hakika wale wanao kuomba ruhusa, hao ndio wanao muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na wakikuomba ruhusa kwa baadhi ya kazi zao, mruhusu umtakaye miongoni mwao, uwaombe msamaha kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁶²

63. Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu anawajua miongoni mwenu wanao ondoka kwa uficho. Basi nawatahadhari wanao khalifu amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu.⁶³

64. Jueni kuwa hakika ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na ardhini. Hakika Yeye anajua mlio nayo. Na siku mtapo rudishwa kwake atawaeleza waliyo yafanya. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.⁶⁴

61 Wenye udhuru kama vile vipofu, viguru, wagonjwa hawana lawama, bali hata nyinyi wazima hamna lawama kula katika nyumba za watoto wenu, kwani hizo ni nyumba zenu. Wala kula katika nyumba za baba zenu, na mama zenu, na ndugu zenu wanaume na ndugu zenu wanawake, au nyumba za ami zenu, au mashangazi zenu, au wajomba zenu, au mama wadogo, dada wa mama zenu, au nyumba ambazo mmewakilishwa kuzitazama, au nyumba za rafiki zenu mnao changanyika nao, ikiwa hamna yaliyo harimishwa humo. Na hayo ikijuulikana kuwa mwenye nyumba ameruhusu yeye au mkewe. Wala hapana ubaya kula humo pamoja au mbali mbali. Na muingiapo katika nyumba toeni salamu kwa waliomo ambao hao ni baadhi yenu kwa umoja wa Dini na ujamaa. Kwani hao ni kama nyinyi. Na maamkio haya ni maamkio yaliyo wekewa Sharia, yenye baraka na thawabu, na pia ndani yake nyoyo hupoa. Na kwa mfano kama huu Mwenyezi Mungu anazifafanua Aya kwa ajili yenu mpate kuelewa waadhi na hukumu ziliomo ndani yake, na mpate kuzifahamu na mzitende.

62 Hakika Waumini wenye kusadiki ni wale ambao wamemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wala hawamwachi Mtume peke yake katika jambo muhimu linalo hitajia wajumuike pamoja kwa ajili yake, kama mfano wa Jihadi. Ila baada ya kumtaka ruhusa ya kuondoka na wakakubaliwa, hakika wanao kukadiri wewe, ewe Nabii, kama unavyo stahiki, na wanatambua umuhimu wa huo mkusanyiko hawaondoki ila baada ya wewe kukubali. Hao ndio wenye kusadiki katika Imani yao kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Basi wakikutaka ruhusa hawa kwenda kufanya baadhi ya maslaha yao mpe ruhusa umtakaye katika wao, pindi ukimwona kuwa ana haja kweli ya kuondoka, na si dharura kwa mkutano kuwapo yeye. Juu ya hivyo waombe maghfira kwa Mwenyezi Mungu kwa kuondoka kwao, ambako kwa hakika hakuelekei kabisa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa maghfira na rehema.

63 Fanyeni hima kuhishimu wito wa Mtume kukuiteni kukusanyika kwa mambo muhimu. Na muitikieni huo wito wake, wala msifanye wito huo kama mnavyo itana nyinyi kwa nyinyi, kuwa inafaa kupuuzza na kuondoka mpendavyo. Wala msiondoke ila baada ya kutaka ruhusa na mkakubaliwa, na tena iwe katika mipaka ya ufino kabisa, na dharura za shida. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* anawajua wanao ondoka bila ya idhini wakijificha ficha kati ya watu ili ati Mtume asiwaone. Na watahadhari wanao kwenda kinyume na amri ya Mwenyezi Mungu asije *Subhanahu* akawapatiliza kwa uasi wao wakapata mateso makali duniani kama ukame na mitetemeko, au akawapa adhabu yenye wingi wa uchungu aliyo waandalia Akhera, nayo ni ya Motoni.

64 Zindukaneni enyi watu! Mjue kuwa Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kumiliki mbingu na ardhi, na viliomo ndani yao. Anayajua mlio nayo, ukafiri wenu na Uislamu wenu, na uasi wenu, na ut'iifu wenu. Basi msiende kinyume na amri yake. Na Yeye atawapa khabari watu, watapo rejea kwake Siku ya Kiyama, kwa yote waliyo yatenda duniani, na atawalipa kwayo. Kwani Yeye amekizunguka kila kitu kwa ujuzi wake.

Sura 25 - Al-Furqan

Utangulizi

Idadi ya Aya za Sura hii ni 77. Zote ni za Makka isipo kuwa Aya 68, 69 na 70.

Sura imeanzia kwa kubainisha cheo cha Qur'ani, na ukubwa wa ufalme wa Mwenye kuiteramsha ambaye ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Na juu ya utukufu wa utawala wake, washirikina bado badala yake wanaabudu masanamu, na wanaikadhibisha Qur'ani, na wanaukataa Utume wa Mtume s.a.w. kwa hoja ya kuwa ati yeye ni binaadamu, anakula chakula, na anatembea masokoni, na kwa ubishi wanataka Malaika ndio wawaletee Ujumbe. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu amewafanya Mitume wake Malaika angeli wafanya ni watu ili wapate kufahamiana na watu. Ubabaishi unge baki. Na wakapinga kwa nini Qur'ani ikawa inateremka vipande vipande. Wakajibiwa hikima ya hayo. Na inda hii ikafuatilizwa kwa mifano yenye kueleza khabari za Mitume waliyo pita na kaumu zao. Lakini hizo kaumu zikafuata matamano yao. Wakawa kama wanyama au wapotovu zaidi katika mwendo wao. Na zikaja Aya za uumbaji zenye kuonyesha ukamilifu wa kudra yake Mtukufu, yenye kufahamisha uangalizi na maarifa. Na Sura ikakhitimisha kwa kutaja sifa za Waumini zitazo warithisha vyumba vya Peponi vya juu, watapo pokewa kwa maamkio na kusalimiwa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ametukuka aliye teremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.¹
2. Ambaye ni wake ufalme wa mbingu na ardhi, wala hakuwa na mwana, wala hakuwa na mshirika katika ufalme, na akaumba kila kitu na akakikadiria kwa kipimo.²
3. Na wamechukua badala yake miungu ambayo haiumbi chochote, bali hiyo inaumbwa, haijamilikii nafsi zao madhara wala manufaa, wala haimiliki mauti, wala uhai, wala kufufuka.³
4. Na wamesema walio kufuru: Haya si chochote ila ni uzushi alio uzua, na

1 Mambo ya Mwenyezi Mungu yametukuka, na kheri yake imezidi. Yeye ndiye aliye iteremsha Furqani, yaani Qur'ani, ya kufarikisha baina ya kweli na uwongo juu ya mja wake, Muhammad s.a.w., ili awe mwonyaji na mwenye kuifikisha hiyo Qur'ani kwa walimwengu wote.

2 Yeye *Subhanahu* ndiye peke yake aliye miliki mbingu na ardhi, aliye takasika na haja ya kuwa na mwana, wala hakuwa na mshirika wowote katika ufalme wake. Na Yeye kaumba kila kitu na akakipima kwa kipimo baraabara kwa sharia zake ili kiweze kutimiza waajibu wake kwa nidhamu. (*Tazama* Maelezo 25:2)

3 Na juu ya yote hayo makafiri wakaacha kumuabudu Yeye, wakenda kuchukua miungu mingine kuiabudu badala ya Mwenyezi Mungu, katika masanamu, na nyota, na watu. Na hao hawanalo waliwezalo kuliumba, bali wao ni viumbe vya Mwenyezi Mungu. Wala hawawezi kujikinga nafsi zao na madhara, wala kujiletea kheri. Wala hawawezi kumfisha yeyote wala kumhuisha, wala kuwafufua maiti kutoka makaburini kwao. Na kila asiye miliki lolote katika hayo basi hastahiki kuabudiwa. Na mjinga wa kutupwa anaye waabudu. Mwenye kustahiki kuabudiwa ni yule Mwenye kumiliki haya yote.

wamemsaidiakwa haya watu wengine! Hakika hawa wamekuja na dhulma na uwongo.⁴

5. Na wakasema: Hivi ni visa vya watu wa kale alivyo viandikisha, anavyo somewa asubuhi na jioni.⁵

6. Sema: Ameyateremsha haya ajuaye siri za katika mbingu na ardhi. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.⁶

7. Na wakasema: Ana nini Mtume huyu? Anakula chakula, na anatembea masokoni! Mbona hakuteremshiwa Malaika akawa mwonyaji pamoja naye?⁷

8. Au akaangushiwa khazina juu yake, au akawa na bustani ale katika hiyo? Wakasema madhaalimu: Nyinyi hamumfuati ila mtu aliye rogwa.⁸

9. Tazama jinsi wanavyo kupigia mifano. Basi wamepotea, wala hawataiweza Njia.⁹

10. Ametukuka ambaye akitaka atakujaalia yaliyo bora kuliko hayo, nayo ni mabustani yapitayo mito kati yao, na atakujaalia majumba ya fakhari.¹⁰

11. Bali wanaikanusha Saa (ya Kiyama). Na Sisi tumemuandalia Moto mkali kabisa huyo mwenye kuikanusha Saa.¹¹

12. Ule Moto ukiwaona tangu mahali mbali wao watasikia hasira yake na mngurumo wake.¹²

4 Makafiri wakaitia ila Qur'ani, wakasema kuwa hiyo ati ni uwongo kaulia Muhammad mwenyewe, na akamsingizia Mwenyezi Mungu. Na wakamsaidia baadhi ya jamaa wengine katika Ahli-l-Kitab. Basi hawa makafiri wamefanya dhulma kwa kauli yao hiyo katika hukumu na kuishambulia Haki, wakaleta uzushi usio kuwa na ushahidi wowote. Kwani hao wanao waashiria katika Ahli-l-Kitab lugha yao hata si Kiarabu. Na Qur'an ni kwa lugha ya Kiarabu fasihi.

5 Wakaisema Qur'ani pia kuwa ati ni uwongo walio andika watu wa kale katika vitabu vyao, kisha akawataka wao wamuandikie na wamsomee asubuhi na jioni mpaka ahifadhi na apate kusema naye hayo hayo.

6 Ewe Nabii! Waambie: Hakika Qur'ani ameyateremsha Mwenyezi Mungu ambaye anazijua siri zilizo fichikana katika mbingu na ardhi. Na ameziweka katika Qur'ani ya muujiza kuwa ni dalili ya kwamba hiyo ni Ufunuo wake *Subhanahu*. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa maghfira na rehema, anawasamehe wenye kuasi pindi wakitubu, wala hafanyi haraka kuwaadhibu.

7 Wakamkejeli Muhammad, wakasema: Kitu gani kinacho mtengua huyu anaye dai kuwa ni Mtume, hata anakula chakula kama tulavyo sisi, na anazururuka masokoni kutafuta maisha kama watu wengine? Angeli kuwa ni Mtume Mwenyezi Mungu angeli mtosheleza kwa hayo, na yeye angeli mwomba Mola wake Mlezi amteremshie Malaika kutoka mbinguni amsaidie katika uwonyaji na kufikisha Ujumbe, na amsadikishe katika wito wake, tupate sisi kumuamini.

8 Na hebu lau angeli mtaka amtosheleze chakula cha kutosha asihitajie kuzunguka masokoni, akamtupia khazina kutoka mbinguni ya kutumia, au akamjaalia na bustani ya kumlisha matunda yake? Na wakubwa wa makafiri walio jidhulumu nafsi zao kwa ukafiri, wenye kuwapotoa watu wasimuamini Muhammad, na wenye kufanya hila za kuwaingiza shaka Waumini, walisema: Nyinyi hamumfuati ila huyu mtu aliye zugwa akili yake, basi anabwabwatika bila ya kuwa na hakika.

9 Hebu angalia, ewe Nabii! Vipi wanavyo kupigia mifano hawa! Mara wanakupigia mfano wa mwenye kurogwa, mara nyengine kuwa ati ni mwendawazimu, mara ya tatu kuwa ni mwongo, na mara yane kuwa unaipokea Qur'ani kutokana na wasio kuwa Waarabu. Hao kwa hayo hakika wameipotea njia ya haki, na kuhojiana kulio sawa. Basi hawaitambui njia ya kufikilia yote hayo.

10 Mwenyezi Mungu ametukuka, na izidi kheri yake! Yeye ndiye ambaye pindi akitaka atakujaalia duniani bora kuliko hayo wanayo pendekeza wao. Kwa Akhera Yeye amekwisha kujaalia kama alivyo kuahidi, nayo ni mabustani mengi yapitayo mito pembezoni mwake, na baina ya miti yake, na majumba ya fakhari madhubuti.

11 Na kwa hakika hawa wamepinga kila Ishara. Kwani wao wamekanusha kufufuliwa, na Siku ya Kiyama. Nao kwa hivyo wanayatia ila matakwa haya ili kuwageuza watu washughulikia upotofu wao. Na Sisi tumekwisha waandalia wanao ikanusha Siku ya Kiyama Moto wenye kuwaka vikali mno.

12 Wakiuona Moto, na huo Moto ukawaona, wataisikia sauti yenye hasira, yenye hamu kuwateketeza.

13. Na watakapo tupwa humo mahali dhiki, hali wamefungwa, wataomba wafe.¹³
14. Msiombe kufa mara moja tu, bali mfe mara nyingi!¹⁴
15. Sema: Je! Haya ni bora au Pepo ya milele, ambayo wameahidiwa wachamngu, iwe kwao malipo na marejeo?¹⁵
16. Watayapata humo wayatakayo daima dawamu. Hii ni ahadi juu ya Mola wako Mlezi, inayo ombwa.¹⁶
17. Na siku atakapo wakusanya wao na hao wanao waabudu, na akasema: Je! Ni nyinyi mlio wapoteza waja wangu hawa, au wao wenyewe walipotea njia?¹⁷
18. Watasema: *Subhanak*, Umetakasika na upungufu! Haikutupasiasisi kuchukulia walinzi badala yako, lakini Wewe uliwastarehesha wao na baba zao hata wakasahau kukumbuka, na wakawa watu walio angamia.¹⁸
19. Basi walikukanusheni kwa mliyo yasema. Kwa hivyo hamwezi kujiondolea wala kujisaidia. Na atakaye dhulumu miongoni mwenu tutamwonjesha adhabu kubwa.¹⁹
20. Na hatukuwatuma kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakenda masokoni. Na tumewajaalia baadhi yenu wawe ni majaribio kwa wengine; je! Mtasubiri? Na Mola wako Mlezi ni Mwenye kuona.²⁰

Na katika hayo ni mfano wa mingurumo inayo toka kifuani mwa aliye kasirika kuwa ni alama ya ukali alio nao.

13 Na watapo tupwa katika pahali pembamba kwa kulingana na unene wao, nao wamefungwa pingu mikono yao kwenye shingo zao, watapiga kelele kuhimiza wateketezwe upesi upesi ili wapate kupumzika na kitisho cha adhabu.

14 Wataambiwa kwa kuwahizi na kuwakejeli: Msitake kuangamia mara moja tu, bali takeni muangamie mara nyingi. Hamtopata kusalimika na hayo mliyo nayo. Na hakika namna ya adhabu zao ni nyingi.

15 Ewe Nabii! Waambie makafiri: Je! Marejeo haya waliyo ahidiwa makafiri ni bora au Pepo yenye kudumu neema zake, na ambayo wameahidiwa Waumini, wachamngu, kuwa itakuwa yao kama ndio malipo na marejeo ya kwenda baada ya kufufuliwa na kuhisabiwa?

16 Humo watapata wakitakacho, wataneemeshwa kwa neema za daima, zisio katika. Na neema hizi ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kwao. Walimwomba Mola wao Mlezi itimie, naye akawaitikia kwa walio liomba; kwani ahadi yake hayendi kinyume.

17 Na taja, kwa ajili ya mawaidha, Siku ambayo Mwenyezi Mungu atawakusanya washirikina kwa ajili ya hisabu katika Siku ya Kiyama, pamoja na hao ambao walikuwa wakiwaabudu duniani badala ya Mwenyezi Mungu, kama Yesu (Isa), Ezra (Uzair) na Malaika. Mwenyezi Mungu atawauliza hao waabudiwa: Je! Ni nyinyi ndio mlio wapoteza waja wangu, mkawaamrisha wakuabuduni, au wao wenyewe ndio walio potea Njia kwa khiari yao, wakakuabuduni?

18 Jawabu yao itakuwa: Umetakasika, na Umetukuka! Haikutafalia sisi kabisa tumtake mlinzi badala yako atunusuru na aangalie mambo yetu. Basi itakuwaje juu ya haya tumtake yeyote atuabudu sisi badala yako Wewe? Lakini sababu ya ukafiri wao hawa ni kuwa uliwastarehesha kwa muda mrefu duniani, wao na baba zao. Hayo yakawapandisha kichwa, wakasahau kukushukuru, na kukuelekea Wewe tu kwa ibada. Basi wakawa kwa jeuri hiyo na ukafiri huo wanastahiki kuangamizwa.

19 Wataambiwa wenye kuabudu, washirikina: Wamekukadhibisheni hao mlio kuwa mkiwaabudu, ambao mkidai kuwa wamekupotezeni. Basi nyinyi leo mnarejea kwenye adhabu. Hamna hila ya kuepukana nayo; wala hamyapati manusura ya kukutoeni. Na wajue waja wote kwamba mwenye kudhulumu kwa ukafiri na uasi kama walivyo fanya hao basi Sisi tutawaadhibu adhabu kali.

20 Na ikiwa washirikina wanakutia ila ewe Nabii, kwa kula kwako chakula, na kwenda kwako masokoni kwa ajili ya kazi na kuchuma maisha, basi huo ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu kwa Mitume wake walio kuja kabla yako. Hatukumtuma yeyote kati yao ila alikuwa akila chakula, na anakwenda kwenda masokoni. Na enyi watu! Tumewafanya baadhi yenu wawe ni mitihani kwa wengine. Na mafisadi wanafanya hila kuziba Njia ya Uwongofu na Haki kwa namna mbali mbali. Basi, enyi Waumini, mtavumilia juu ya Haki yenu, na mtaishikilia Dini yenu, mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake kwa ushindi? Subirini! Kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuvizunguka vitu vyote, na atamlipa kila mtu kwa kitendo chake

- 21.** NA WALISEMA wale wasio taraji kukutana nasi: Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika au hatumwoni Mola wetu Mlezi? Kwa yakini hawa wamejiona bora nafsi zao, na wamepanda kichwa vikubwa mno!²¹
- 22.** Siku watakayo waona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wakosefu. Na watasema: Mungu apishe mbali!²²
- 23.** Na tutayaandea yale waliyo yatenda katika vitendo vyao, tuvifanye kama mavumbi waliyo tawanyika.²³
- 24.** Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makaazi bora na mahali penye starehe nzuri.²⁴
- 25.** Na siku zitapo funguka mbingu kwa mawingu, na wateremshwe Malaika kwa wingi,²⁵
- 26.** Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa *Arrahman*, Mwingi wa Rehema, na itakuwa siku ngumu kwa makafiri.²⁶
- 27.** Na siku ambayo mwenye kudhulumu atajiuma mikono yake, na huku anasema: Laiti ningeli shika njia pamoja na Mtume!²⁷
- 28.** Ee Ole wangu! Laiti nisingeli mfanya fulani kuwa rafiki!²⁸
- 29.** Amenipoteza, nikaacha Ukumbusho, baada ya kwisha njia, na kweli Shet'ani ni khaini kwa mwanaadamu.²⁹
- 30.** Na Mtume alikuwa akisema: Ee Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wameifanya hii Qur'ani ni kihame.³⁰
- 31.** Na vivi hivi tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wakosefu, na Mola wako

21 Na wakasema wanao kataa kufufuliwa na wala hawatamai kuwa yapo malipo kwa vitendo vyao: Kwa nini hatuteremshiwi Malaika wa kukuunga mkono, au Mwenyezi Mungu akajionyesha kwetu na akatwambia kwamba kweli Yeye kakutumama? Kiburi kimeyajaa katika nafsi zao, na wamepita mpaka katika udhalimu na ujabari!

22 Siku ya Kiyama watawaona Malaika kama walivyo tamani, na hayo yatakuwa ni sababu ya kitisho kwao wala si jambo la kuwafurahisha. Watatafuta kujilinda nao, kama walivyo kuwa wakitafta kujilinda na vinavyo watisha duniani.

23 Na Siku ya Kiyama tutawaletea waliyo yatenda katika mambo ya kuonyesha wema kwa dhaahiri na hisani katika dunia, na Sisi tutayafanya yaondokee patupu, na tutawaharimisha thawabu zake, kwa kuwa yamekosa Imani ambayo ni dharura ipatikane ili vitendo vitiwe maanani.

24 Watu wa Peponi Siku ya Kiyama ndio watao kuwa na utulivu bora, na mashukio mazuri, na makaazi ya starehe, kwa sababu hii ni Pepo walio andaliwa Waumini, si Moto walio andaliwa makafiri.

25 Ewe Nabii! Itaje Siku itapo pasuka mbingu na ikafunguka, na yakadhihiri kati yake mawingu, na Malaika wakashuka khasa kwa yakini.

26 Katika siku hii mali ya watu wenye mali yataharibika, madai yao wanao jidai yatakatika, na Ufalme wote utabaki ni wa *Arrahmani*, Mwingi wa Rehema, peke yake. Na itakuwa siku ya shida ngumu mno kwa makafiri.

27 Siku ya Kiyama mwenye kujidhulumu nafsi yake atajiuma mikono yake kwa hasira na majuto kwa ukafiri wake na kumwenda kinyume Mtume, na kwa kutamani atasema: Laiti lau ningeli mfuata Mtume, nikaifuata njia ya kwendea Peponi, na nikaiepuka njia ya kwendea Motoni!

28 Na atasema kwa kujuta kuwafuata walio mpoteza: Laiti ningeli kuwa sikumsadiki fulani, ambaye nimemwachia aniongoze.

29 Rafiki huyu amenibaidisha na Ukumbusho, Dhikr, kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kuikumbuka Qur'ani baada ya kwisha kuwa ni nyepesi kwangu. Ndio hivi Shetani anavyo mkhini binaadamu, na kumtokomeza kwenye hilaki yake.

30 Na Mtume alisema akimshitakia Mwenyezi Mungu kwa taabu anazo zipata kwa watu wake: Hakika hawa wameiacha Qur'ani na wameihama, na wameshikilia katika kuipuuza, na kuifanyia inda na uadui.

Mlezi anatosha kuwa Mwenye kuongoa na Mwenye kunusuru.³¹

32. Na wakasema walio kufuru: Kwa nini hakuteremshiwa Qur'ani kwa jumla moja? Hayo ni hivyo ili tuuthibitisha moyo wako, na ndio tumeisoma kwa mafungu.³²

33. Wala hawatakuletea mfano wowote, ila na Sisi tutakuletea (jawabu) kwa haki, na tafsiri iliyo bora.³³

34. Wale ambao watakao kusanywa na kubururwa kifudifudi mpaka kwenye Jahannamu, hao watakuwa na mahali pabaya, ndio wenye kuipotea sana njia.³⁴

35. Na hakika tulimpa Musa Kitabu na tukamweka pamoja naye nduguye, Harun, kuwa waziri.³⁵

36. Tukawaambia: Nendeni kwa watu walio kanusha Ishara zetu. Basi tukawateketeza kabisa.³⁶

37. Na watu wa Nuhu, walipo wakanusha Mitume, tuliwazamisha, na tukawafanya ni Ishara kwa watu. Na tumewaandalia wenye kudhulumu adhabu chungu.³⁷

38. Na tuliwaangamiza kina A'di na Thamudi na watu wa Rass na vizazi vingi vilivyo kuwa kati yao.³⁸

39. Na wote tuliwapigia mifano, na wote tuliwaangamiza kabisa kabisa.³⁹

40. Na kwa yakini wao wanafika kwenye nchi ilio teremshiwa mvua mbaya. Basi, je, hawakuwa wakiiona? Bali walikuwa hawataraji kufufuliwa.⁴⁰

41. Na wanapo kuona hawakuchukulii ila ni mzaha tu, na (wanasema): Ati ndiye huyu

31 Kama tulivyo wajaalia watu wako, ewe Muhammad, wanavyo kufanyia uadui na kukukadhibisha, basi kadhaalika tulimjaalia kila Nabii ana maadui miongoni mwa wakosefu, wanao mfanyia uadui na wanaupinga wito wake. Na Mwenyezi Mungu atakunusuru, na atakuongoa mpaka uwashinde. Na Yeye anakutosha kwa uwongofu na kukunusuru.

32 Na makafiri kutaka kuikibehe Qur'ani walisema: Kwa nini haikuteremshwa kwa mara moja? Na Sisi hakika tumeiteremsha kwa mapande mapande ili moyo wako uthibiti kwayo kwa raha yako na ili uihifadhi. Na tumeisoma, yaani tumeigawa kwa Aya, au tumeisoma kwa ulimi wa Jibril, kidogo kidogo kwa utulivu na upole.

33 Na wala hawakujii na upinzani dhaifu, ila nasi tunakuletea Haki ya kubainisha, na bora ya maelezo.

34 Na walio ukataa Ujumbe wako watabururwa kupelekwa Motoni kifudifudi na madhalili. Hao ndio watu wa chini kabisa kwa cheo, na ndio walio zama mno katika upotovu.

35 Na Mtume s.a.w. anapozwa kwa yaliyo wapata Mitume wa kabla yake. Hakika Sisi tulimteremshia Musa Taurati, na tukamkalifisha afikishe Ujumbe wetu, na tukamuunga mkono kwa ndugu yake Harun, awe waziri wake na msaidizi katika kazji yake.

36 Tukasema: Nenda wewe na nduguyo kwa Firauni na watu wake. Tukamuunga mkono kwa miujiza inayo onyesha ukweli wake. Hawakumuamini, wakamkadhibisha. Mwisho wao ukawa tukawateketeza na tukawafutilia mbali!

37 Hali kadhaalika kabla ya Musa tuliwafanyia kaumu ya Nuhu walipo mkadhibisha, na aliye mkanusha Mtume mmoja basi amewakanusha Mitume wote. Nao tukawazamisha katika tufani, na tukawafanya wawe ni zingatia kwa watu. Na tukawajaalia hao na kila mshirikina kupata adhabu chungu Akhera.

38 Na kadhaalika tuliwahiliki A'di na Thamudi na watu wa Rass walipo wakanusha Mitume wao. Na tuliziangamiza kaumu nyingi baina ya kaumu ya Nuhu na baina ya A'di, yakawapata malipo ya wenye kudhulumu. (*Tazama* Maelezo 25:38)

39 Na Sisi tumeziona kaumu zote hizi. Tukawakumbusha mawaidha, na mifano ya kweli yenye manufaa. Lakini hawakuwaidhika. Tukawashika wote kwa kuwadhibu, tukawahiliki, na tukayabomoa majumba yao mpaka kifusi.

40 Na hawa Makureshi katika safari zao za kwenda Sham wanapita kwenye mji wa kaumu Lut'i, tulio unyeshea mvua ya shari na ovu kabisa, nayo ni mawe ya Motoni. Je! Hawaoni mji huo wakawaidhika kwa yaliyo wafika watu wake? Hakika wao wanauona huo, lakini si kwa macho ya kuwaidhika na kuzingatia. Kwani hawaamini ahadi (za Mwenyezi Mungu) wala kufufuliwa. Wala hawataraji kuwa ipo siku watakuja fufuliwa kwa ajili ya hisabu.

Mwenyezi Mungu aliye mtuma kuwa Mtume?⁴¹

42. Kwa hakika alikuwa karibu kutupoteza tuiache miungu yetu, ingeli kuwa hatukushikamana nayo kwa kuvumilia. Bado watakuja jua, watakapo iona adhabu, ni nani aliye potea njia.⁴²

43. Je! Umemwona aliye yafanya matamania yake kuwa ndio mungu wake? Basi je, wewe utakuwa ni wakili wake?⁴³

44. Au wewe unadhani kwamba wengi wao wanasikia au wanaelewa? Hao hawakuwa ila ni kama nyama hoa tu, bali wao wamepotea zaidi njia.⁴⁴

45. Je! Huoni jinsi Mola wako Mlezi anavyo kitandaza kivuli. Na angeli taka angeli kifanya kikatulia tu. Kisha tumelifanya jua kuwa ni kiongozi wake.⁴⁵

46. Kisha tunakivutia kwetu kidogo kidogo.⁴⁶

47. Naye ndiye aliye kufanyieni usiku kuwa ni vazi, na usingizi kuwa mapumziko, na akakufanyieni mchana ni kufufuka.⁴⁷

48. Naye ndiye anaye zituma pepo kuwa bishara njema kabla ya rehema yake, na tunayateremsha kutoka mbinguni maji safi.⁴⁸

49. Ili kwa hayo tuihuishe nchi iliyo kufa, na tuwanyweshe wanyama na watu wengi tulio waumba.⁴⁹

41 Na wakikuona watu hawa hawakuchukulii ila kukufanyia kejeli na maskhara. Na huambiana wao kwa wao: Ndiye huyu aliye mtuma kwetu Mwenyezi Mungu awe ni Mtume, na sisi tumfuate twende nyuma yake?

42 Mtu huyu hakika kajaaliwa kuwa na ufasihi mzuri, na hoja za kuvutia kwa wanao msikia. Na hapana shaka ameweza kuchota katika imani zetu hata alikaribia kututoa kwa miungu yetu tumfuate mungu wake. Lakini sisi tumesimama imara juu miungu yetu na dini yetu. (Mwenyezi Mungu anasema:) Tutakuja wabainishia ukweli wa mambo watapo kuja iona adhabu Siku ya Kiyama, na watajua nani huyo aliye thibiti katika upotovu na makosa.

43 Ewe Mtume! Umeona upotovu wa mwenye kufuata matamania yake na pumbao lake hata akawa anaabudu mawe ambayo hayadhuru wala hayanafiishi? Na wewe umetumwa uwe mwonyaji na mbashiri, wala hukuwakilishwa kwa imani yao na uwongofu wao.

44 Na hivyo unadhani kuwa wengi wao wanasikia kwa sikio la kufahamu au wanaongoka kwa akili zao? Wamesha tupilia mbali kama walivyo amrisha na ndoto zao. Wamekuwa kama wanyama wa kufuga, hawanalo linalo washughulisha ila kula, na kunywa, na kustarehe na maisha ya dunia. Wala hawana fikra yoyote baada ya hayo. Bali hali yao ni ovu zaidi kuliko ya wanyama, kwani wanyama huwafuata bwana zao katika yenye kheri nao, na wanayaepuka ya kuwadhuru. Lakini watu hawa wanajitokomeza wenyewe kwenye mambo ya kuwahiliki

45 Tumesimamisha dalili za Tawhidi, Upweke wa Mwenyezi Mungu, za kuwaongoa wenye akili. Hebu kiangalie kivuli. Mwenyezi Mungu amekitandaza na akakifanya kimetulia mwanzo wa mchana. Kisha tukalipeleka jua likaondoa pahala pake kwa mwako wake. Likawa jua ni kama ndio linaongoza kivuli. Bila ya jua, kivuli kisingeli juulikana. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu ange penda angeli kifanya kivuli kitulie vile vile kimewang'ang'ania watu, na yakawaharibikia maslaha yao na mambo yao. (*Tazama Maelezo 25:45*)

46 Na kukiondoa kwetu kivuli ni kwa utaratibu, kwa kipimo. Hakukuwa kwa mara moja. Na katika hayo yapo manufaa kwa watu.

47 Na katika Ishara za Tawhidi ni kuwa tumeufanya usiku ni sitara kwa kiza chake, ndani yake wanaingia viumbe ukawazunguka kama inavyo wazunguka nguo kwa mwenye kuivaa. Na tukawatengeneza malazi, ikawa ni mapumziko kupumzika na machofu, na kwa mwangaza wa jua wanazinduliwa watu watafute maisha yao na riziki zao.

48 Na Yeye ndiye aliye zifanya pepo zimumikie, zikasukuma mawingu, nayo yakwabashiria watu itakuja mvua, ambayo ni rehema itokayo kwake kuwaendea wao. Na hakika Sisi tunateremsha kutoka mbinguni maji safi yanayo safisha kuondoa najisi na uchafu. (*Tazama Maelezo 25:48*)

49 Tunaiteremsha mvua kwa sababu makulima yapate kumea na kukua, na ardhii ipate kufufuka baada ya

50. Na kwa yakini tumeisarifu kati yao wapate kukumbuka. Lakini watu wengi wanakataa ila kukufuru.⁵⁰
51. Na tungeli taka tungeli peleka katika kila mji Mwonyaji.⁵¹
52. Basi usiwaṭ'ii makafiri. Na pambana nao kwayo kwa Jihadi kubwa.⁵²
53. Naye ndiye aliye zipeleka bahari mbili, hii tamu mno, na hii ya chumvi chungu. Na akaweka baina yao kinga na kizuizi kizuiacho.⁵³
54. Naye ndiye aliye muumba mwanaadamu kutokana na maji, akamjaalia kuwa na nasaba na ushemeji. Na Mola wako Mlezi ni Muweza.⁵⁴
55. Na wanayaabudu badala ya Mwenyezi Mungu yasiyo wafaa wala yasiyo wadhuru. Na kafiri daima ni msaidizi wa kumpinga Mola wake Mlezi.⁵⁵
56. Nasi hatukukutuma ila kuwa ni Mbashiri na Mwonyaji.⁵⁶
57. Sema: Sikukuombeni ujira juu yake; ila atakaye na ashike njia iendayo kwa Mola wake Mlezi.⁵⁷
58. Na mtegemee Aliye Hai, ambaye hafi. Na umtukuze kwa sifa zake. Na yatosha kwake kuwa yeye ni Mwenye khabari za dhambi za waja wake.⁵⁸
59. Ambaye ameziumba mbingu na ardhi, na viliomo ndani yake kwa siku sita. Kisha akatawala juu ya A'rshi, *Arrahman*, Mwingi wa Rehema! Uliza khabari zake kwa wamjuaye.⁵⁹
60. Na wanapo ambiwa: Msujudieni *Arrahman*! Wao husema: Ni nani *Arrahman*? Je!

kufa kwake, na wanyeshwe watu na wanyama walio umbwa.

50 Na hii Qur'ani tumeibainisha na tumeisarifu, tumeifanya, ili watu wamkumbuke Mola wao Mlezi, na wawaidhike, na watende kwa mujibu wake. Lakini wengi wa watu wanakataa isipo kuwa ukafiri na inda tu

51 Na lau kuwa tumetaka basi tungeli mpeleka mwonyaji kwenye kila mji. Basi jitahidi na wito wako; na wacha maneno ya makafiri; na tupilia mbali wanayo yaleta.

52 Na endelea na kulingania kwako kwa Haki, na kufikisha Ujumbe wa Mola wako Mlezi. Na wao wakiupinga wito wako, na wakawavamia Waumini basi wapige vita, na kwa hayo pigana Jihadi kubwa.

53 Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye ziendesha bahari mbili, bahari ya maji matamu na bahari ya maji ya chumvi. Na akafanya njia ya kila moja inakaribiana na nyengine. Na juu ya hivyo maji yao hayachanganyikani. Hiyo ni neema na rehema kwa watu. (*Tazama* Maelezo 25:53)

54 Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye umba kutokana na manii hawa watu, na akawajaalia wanaume na wanawake walio khusiana kwa nasaba ya kuzaana na kwa ushemeji wa kuoana. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza kwa atakayo, kwani kwa hiyo hiyo manii ameumba namna mbili mbali.

55 Na baada ya Ishara hizi zenye kuonyesha kuwa Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anaye stahiki kuabudiwa, na kwamba hapana mungu isipo kuwa Yeye, wanatoka kikundi cha watu kuabudu masanamu yasiyo wafaa wala kuwadhuru. Na hawa kwa kujua kwao haya wanamsaidia Shetani, na yeye anawapoteza. Basi hao inakuwa wanasaidiana katika kuipinga Haki ambayo Mwenyezi Mungu anawaitia.

56 Na ewe Nabii! Huna jukumu ila kufikisha hayo ulio tumwa basi, na kuwabashiria Pepo Waumini, na kuwakhofisha makafiri kwa haya watayo yakuta. Baada ya hayo huna jengine unalo takiwa.

57 Na waambie: Hakika mimi sitafuti kwa huku kukuiteni muufuate Uislamu ujira wowote wala malipo. Ila nilitakalo ni mwongoke na muifuate Njia ya Haki mrejee kwa Mola wenu Mlezi.

58 Na katika mambo yako mtegemee Mwenyezi Mungu Aliye Hai, ambaye hayumkini kufa. Na mtakase na mtukuze kwa kuzisifu neema zake. Na waachilie mbali walio toka kwenye Njia. Kwani Mwenyezi Mungu anawajua vyema, na atawalipa kwa dhambi zao.

59 Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi na vilio baina yao kwa siku sita. Naye ametawala juu ya A'rshi, Kiti cha Enzi, cha Ufalme wote, na madaraka yake yameenea kila kitu. Na Yeye ndiye Mwingi wa Rehema, *Arrahman*. Na ukitaka lolote katika sifa zake muulize ajuae atakujibu. Naye ni Mwenyezi Mungu Mwenye hikima. (*Tazama* Maelezo 25:59)

Tumsujudie unaye tuamrisha wewe tu? Na huwazidishia chuki.⁶⁰

61. Ametukuka aliye zijaalia nyota mbinguni, na akajaalia humo taa na mwezi unao ng'ara.⁶¹

62. Naye ndiye aliye fanya usiku na mchana kufuatana kwa nafuu ya anaye taka kukumbuka, au anaye taka kushukuru.⁶²

63. Na waja wa *Arrahman* Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: Salama!⁶³

64. Na wale wanao keshwa kwa ajili ya Mola wao Mlezi kwa kusujudu na kusimama.⁶⁴

65. Na wale wanao sema: Mola wetu Mlezi! Tuondolee adhabu ya Jahannamu. Hakika adhabu yake ikimpata mtu haimwachi.⁶⁵

66. Hakika hiyo ni kituo na makao mabaya.⁶⁶

67. Na wale ambao wanapo tumia hawatunii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo.⁶⁷

68. Na wale wasio mwomba mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawau nafsi aliyo iharimisha Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa haki, wala hawazini - na atakaye fanya hayo atapata madhara,⁶⁸

69. Atazidishiwa adhabu Siku ya Kiyama, na atadumu humo kwa kufedheheka.⁶⁹

70. Isipo kuwa atakaye tubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁷⁰

60 Na wakiambiwa hawa makafiri: Mnyenyekeeni *Arrahmani*, Mwingi wa Rehema, na mumuabdu, wao husema: Nani huyo *Arrahmani*? Sisi hatumjui, hata tumsujudie. Basi tukufuate amri yako tu? Na wanazidi kuwa mbali na kutengeka na Imani.

61 Ametukuka *Arrahman*, Mwingi wa Rehema, na zimezidi fadhila zake. Ameziumba sayari mbinguni na akazijaalia na vituo vyake vya kupitia, na katika hizo akaumba jua kuwa ni taa yenye mwangaza, na mwezi wenye nuru. (Tazama Maelezo 25:61)

62 Mwingi wa Rehema ndiye aliye ufanya usiku na mchana kufuatana, mmoja nyuma ya mwenzie. Na tumeyapanga haya ili mwenye kutaka akumbuke mpango huu, na ajue hikima ya Mwenyezi Mungu na uweza wake; au apate kushukuru kwa neema hii njema.

63 Na waja wa Mwenyezi Mungu ni wale wanao nyenyekea duniani. Wakitembea katika ardhi wanatembea kwa utulivu na staha. Hali kadhaalika katika mambo yao yote. Na masafihi katika washirikina wakiwasubu wanawaachilia mbali na shani yao, na wanawaambia: Hatuna shani nanyi. Letu sisi ni *Assalamu Alaikum!*

64 Na wale ambao wanakesha katika ibada na Sala, wakimdhukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi.

65 Na wale ambao khofu yao inashinda matarajio - nao ndio mwendo wa wachamngu. Basi wanaikhofu adhabu ya Akhera, na hawaachi kumwomba Mwenyezi Mungu awaepusha na adhabu ya Jahannamu. Kwani adhabu yake ikimteremkia mkosefu inamganda, wala haimwachi.

66 Na hakika Jahannamu ni kituo kiovu mno kwa mwenye kutua, na makao maovu kwa mwenye kukaa ndani yake.

67 Na katika alama za waja wa Mwenyezi Mungu ni kuwa wana kiasi katika kutumia kwao mali, kwa ajili ya nafsi zao na jamaa zao. Wao hawafanyi ubadhirifu, wala hawabanii matumizi bila ya kiasi. Bali kutoa kwao ni kati kati baina ya hayo.

68 Na katika sifa zao hao waja wa Mwenyezi Mungu ni kuwa wameisafia niya Tawhid, na wakatupilia mbali kila athari ya ushirikina katika kumuabudu Mola wao Mlezi. Na wakajizua kuuwa nafsi aliyo kataza Mwenyezi Mungu kuuliwa, ila ikiwa imefanya uadui basi huuliwa kwa haki. Nao hujitenga mbali na uzinzi, na katika mambo ya starehe hawatendi ila lilio halali tu, ili waepukane na adhabu ya mambo yanayo angamiza. Kwani anaye tenda katika mambo hayo atakuta shari na adhabu.

69 Na Siku ya Kiyama atapata adhabu mardufu kuliko hiyo, na atadumu Motoni kwa udhalili na unyonge.

70 Lakini mwenye kutubu na madhambi haya na akawa mkweli katika Imani yake, na akafuatiliza hayo kwa ut'iifu na vitendo vyema, hao atawasamehe kwa rehema yake, na atawajaalia bora ya thawabu badala ya maovu yaliyo kwisha tangulia. Na hakika shani ya Mwenyezi Mungu ni kurehemu na kusamehe.

71. Na aliye tubu na akafanya mema, basi hakika huyo ametubu kweli kweli kwa Mwenyezi Mungu.⁷¹
72. Na wale ambao hawatoi ushahidi wa uwongo, na pindi wapitapo penye upuuzi, hupita kwa hishima yao.⁷²
73. Na wale ambao wanapo kumbushwa Ishara za Mola wao Mlezi hawajifanyi viziwi nazo, na vipofu.⁷³
74. Na wale wanao sema: Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na wenetu yaburudishayo macho, na utujaalie tuwe waongozi kwa wachamngu.⁷⁴
75. Hao ndio watakao lipwa makao ya juu kwa kuwa walisubiri, na watakuta humo maamkio na salamu.⁷⁵
76. Wadumu humo - kituo na makao mazuri kabisa.⁷⁶
77. Sema: Mola wangu Mlezi asinge kujalini lau kuwa si kuomba kwenu. Lakini nyinyi mmemkadhibisha. Basi adhabu lazima iwe.⁷⁷

71 Na hivyo ndio mambo yetu yendavyo, yaani kuwa mwenye kutubu madhambi, na akaonyesha matokeo yake katika kukubali ut'iifu na kuepuka maasi, basi huyo Mwenyezi Mungu huikubalia toba yake. Na kwa hivyo hurejea kwa Mola wake Mlezi baada ya kumwacha kwake.

72 Na katika khulka za waja wa Mwingi wa Rehema ni kuwa wanajiepusha na kutoa ushahidi wa uwongo, na wakisadifu kukutana na mtu asiye kuwa na kauli au kitendo chema hawashirikiani naye katika hayo, na huacha kufuatana naye.

73 Na katika sifa zao ni kuwa mwenye kuwaidhi akiwapa mawaidha, na akawasomea Aya za Mwenyezi Mungu, humwelekea kumsikiliza, na nyoyo zao zikawaidhika, na macho yao hufunuka. Wala hawawi kama wale ambao wanatapatapa wanapo yasikia, wanapuza, masikio yao hayapenyi kitu, wala macho yao hayafumbuki.

74 Na wao humwomba Mola wao Mlezi awajaalie wake zao na watoto wao wawe wa kuwapoza moyo kwa vitendo vya kheri, na awajaalie wawe ni waongozi katika kheri ili watu wema wawafuate.

75 Hawa wenye kusifiwa kwa sifa hizi tulizo zitaja ndio waja wa Mwenyezi Mungu wa kweli. Na malipo yao ni makao ya Peponi ya juu, kuwa ni jazaa ya kusubiri kwao juu ya ut'iifu. Na huko Peponi watakuta maamkio, na kusalimiwa.

76 Na neema zao za Peponi ni za daima, hazikatiki. Pepo ndio kituo na makao mema kabisa.

77 Ewe Mtume! Waambie watu: Mwenyezi Mungu hakutakini nyinyi ila mumuabudu Yeye, na mumwombe Yeye katika mambo yenu, wala msimwombe yeyote mwenginewe. Na kwa hayo ndio kakuumbeni. Lakini makafiri katika nyinyi wameyakanusha waliyo kuja nayo Mitume. Basi adhabu yao itawaganda hao, wala hapana wa kuwaokoa nayo.

Sura 26 - Ash-Shu'araa

Utangulizi

Sura hii imeanzia kwa kuisifu Qur'ani yenyewe, ikaingia kuwaonya makafiri kwa uweza wa Mwenyezi Mungu kuwateremshia adhabu juu yao, na kumliwaza Nabii s.a.w. kwa anayo yapata ya kukanushwa na watu wake, kwa kutajiwa yalio wapata Mitume wa kabla yake ya kukadhibishwa na kaumu zao. Ikasimulia mkutano wa Musa na Harun walipo kutana na Firauni, na alivyo wakadhibisha yeye. Kisha *Subhanahu* akataja kisa cha Ibrahim, baba wa Manabii, na khabari za Nuhu pamoja na kaumu yake, na mambo ya A'adi, na Saleh pamoja na Thamud. Kisha ikaelezea Sura wito wa Lut'i na kisa cha Shuaib na watu wa Vichakani (Al-Aykat).

Na mwenye kuzingatia visa vya hawa Manabii saba ataona asili ya wito wao ni mmoja. Na njia ya makafiri katika kupinga ujumbe wao ni moja. Kama ilivyo anzia Sura basi ilikhitimishia mazungumzo kwa kuvunja wazo la kuwa Mtume ni mtunga mashairi, na kuwa Qur'ani ni mashairi.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. T'aa Siin Miim. (T'.S.M.)¹
2. Hizi ni Aya za Kitabu kinacho bainisha.²
3. Huenda labda ukajikera nafsi yako kwa kuwa hawawi Waumini.³
4. Tunge penda tungeli wateremshia kutoka mbinguni Ishara zikanyenyekea shingo zao.⁴
5. Wala hauwafikii ukumbusho mpya kutoka kwa *Arrahman* ila wao hujitenga nao.⁵
6. Kwa yakini wamekanusha; kwa hivyo zitakuja wafikia khabari za yale waliyo kuwa wakiyafanyia mzaha.⁶
7. Je! Hawakuiona ardhi, mimea mingapi tumeiotesha humo, ya kila namna nzuri?⁷

1 Harufi hizi na mfano wa hizi ndizo zikakusanyika kuifanya Qur'ani kuwa ni muujiza ulio washinda watu kuiga mfano wake, ijapo kuwa hizo harufi ndizo wanazo zitamka. Basi mwenye kuitilia shaka hii Qur'ani kuwa imetoka kwa Mwenyezi Mungu au la, basi na alete mfano wake. Na hatoweza.

2 Maneno haya niliyo kufunulia ni Aya za Kitabu chenye kuweka wazi hukumu zote ziliomo ndani yake.

3 Ewe Nabii! Hebu jionee huruma nafsi yako. Usijikere kwa kuhuzunukia inadi ya watu wako, na kuto amini kwao.

4 Sisi tunaweza kuwaletea muujiza wa kuwalazimisha Imani, wat'ii kwa unyenyekevu amri yake, na yatimie unayo yatarajia. Lakini hatuwaletei, kwa sababu mwendo wetu ni kuwaongoza watu waamini bila ya kuwalazimisha, ili isikosekane hikima ya kujaribiwa kwa mitihani, na yanayo kuja baada yake ya thawabu na adhabu.

5 Wala Mwenyezi Mungu hawaletei watu wako kwa ufunuo wake ya kuwakumbusha Dini ya Haki kuwa ni rehema kwao, ila wao huzua upya upinzani na ukafiri kuukataa. Kwani njia ya uwongofu imekwisha zibwa mbele yao.

6 Hawa hakika wamekadhibisha Haki uliyo ileta, na wakaifanyia maskhara. Lakini wewe wasubirie. Wataona matokeo ya maskhara yao ya kuangamiza.

7 Hivyo hao wanatenda watendavyo katika ukafiri wao na kukadhibisha kwao wala hawaangalii baadhi ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu katika hii hii ardhi? Lau kuwa wanaangalia kwa kuzingatia wangeli ongoke. Hebu wazingatie hii mimea ya kila namna yenye manufaa tunayo itoa Sisi kwenye ardhi, na wala

8. Hakika katika haya zipo Ishara. Lakini wengi wao hawakuwa wenye kuamini.⁸
9. Na hakika Mola wako Mlezi ndiye Yeye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.⁹
10. Na Mola wako Mlezi, alipo mwita Musa, akamwambia: Fika kwa watu madhaalimu,¹⁰
11. Watu wa Firauni. Hawaogopi?¹¹
12. Akasema: Hakika mimi nachelea wasinikanushe.¹²
13. Na kifua changu kina dhiki, na ulimi wangu haukunjuki vyema. Basi mtumie ujumbe Harun.¹³
14. Na wao wana kisasi juu yangu, kwa hivyo naogopa wasije kuniuwa.¹⁴
15. Akasema: Siyo hivyo kabisa! Nendeni na miujiza yetu. Hakika Sisi tu pamoja nanyi, tunasikiliza.¹⁵
16. Basi mfikieni Firauni na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹⁶
17. Waachilie Wana wa Israili wende nasi.¹⁷
18. (Firauni) akasema: Sisi hatukukulea wewe utotoni, na ukakaa kwetu katika umri wako miaka mingi?¹⁸
19. Na ukatenda kitendo chako ulicho tenda, nawe ukawa miongoni mwa wasio na shukrani?¹⁹
20. (Musa) akasema: Nilitenda hayo hapo nilipo kuwa miongoni mwa wale waliopotea.²⁰

hawezi hayo isipo kuwa Mungu Mmoja Muweza.

8 Hakika katika kutoka kwa hii mimea ni dalili kubwa ya kuwepo Muumba Muweza. Lakini wengi wa watu si wenye kuamini.

9 Hakika Mwenye kumiliki mambo yako, na Mwenye kukulinda, ndiye atakaye waadhibu hao wanao kadhibisha, na ndiye Mwenye kuwafadhili Waumini kwa rehema.

10 Ewe Muhammad! Watajia watu wako kisa cha Musa pale Mola wako Mlezi alipo mwita: Ewe Musa! Nenda kwa Utume kwa watu walio dhulumu nafsi zao kwa ukafiri, na wakawadhulumu Wana wa Israili kwa kuwafanya watumwa na kuwauwa watoto wao wanaume

11 Nenda kwa kaumu ya Firauni; kwani hao wamepita mipaka katika dhulma yao. Ama ajabu ya watu hawa! Hawaogopi nini litalo wafika kwa vitendo vyao hivi, wakatahadhari?

12 Musa akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Mimi nina khofu wasije kuukataa ujumbe wangu kwa kiburi na inda.

13 Na mimi nimejaa dhiki kwa kuwa wataniambia mwongo, na ulimi wangu si mkunjufu wa kuweza kuhojiana nao kama ninavyo penda. Basi mtume Jibril ende kwa ndugu yangu aje kuniunga mkono katika hii kazi yangu

14 Na watu hawa wana kisasi juu yangu. Kwani mimi nilimuwa mtu katika wao. Basi nina khofu watakuja niuwa kwa kisasi kabla sijatimiza kazi yangu. Hayo yananzidisha khofu.

15 Mwenyezi Mungu akamwambia: Hawatokuuwa. Na kwa mintarafu ya Haruni nimekukubalia ombi lako. Basi nendeni nanyi mmejizatiti na miujiza yetu. Mimi niko pamoja nanyi kwa ulinzi. Nayasikia yanayo jiri baina yenu na Firauni. Nyinyi mtapata ushindi, na kuungwa mkono.

16 Muelekeeni Firauni na mwambieni: Sisi ni Watume wawili tumetumwa na Mola Mlezi wa walimwengu wote.

17 Anakwambia Mola Mlezi wa walimwengu wote: Waachilie huru Wana wa Israili, wende nasi.

18 Firauni akamwambia Musa kwa kumsimbulia, naye alimtambua walipo ingia na wakakadimisha Ujumbe wao, kwani alilelewa mle mle katika kasri lake: Hatukukulea sisi ulipo kuwa mtoto? Na ukaishi chini ya ulezi wetu kwa miaka mingi katika umri wako?

19 Na ukatenda makosa yako ya jinaya maovu kumuwa mtu katika kaumu yangu, na ukazikanusha neema zangu nilizo kufanyia, hukuwahifadhi raia zangu, ukaushambulia ungu wetu kwa kudai kuwa wewe ati ni Mtume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote.

20 Musa akasema: Niliyafanya uliyo yataja kwa kutojua yanayo faa kutambulikana kwa akili nayo ni jambo la kuuwa. Basi hapana masimbulizi juu yangu.

21. Basi nikakukimbieni nilipo kuogopeni, tena Mola wangu Mlezi akanitunukia hukumu, na akanijaalia niwe miongoni mwa Mitume.²¹
22. Na hiyo ndiyo neema ya kunisumbulia, na wewe umewatia utumwani Wana wa Israili?²²
23. Firauni akasema: Na nani huyo Mola Mlezi wa walimwengu wote?²³
24. Akasema: Ndiye Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, na viliomo baina yao, ikiwa nyinyi ni wenye yakini.²⁴
25. (Firauni) akawaambia walio mzunguka: Hamsikilizi?²⁵
26. (Musa) akasema: Ndiye Mola wenu Mlezi, na Mola Mlezi wa baba zenu wa kwanza.²⁶
27. (Firauni) akasema: Hakika huyu Mtume wenu aliye tumwa kwenu ni mwendawazimu.²⁷
28. (Musa) akasema: Ndiye Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi na viliomo baina yao, ikiwa nyinyi mnatia akilini.²⁸
29. (Firauni) akasema: Ukimfuata mungu mwengine asiye kuwa mimi, basi bila ya shaka nitakufunga gerezani.²⁹
30. Akasema: Je! Ijapo kuwa nitakuletea kitu cha kubainisha wazi?³⁰

21 Nikakukimbieni nilipo khofu kuwa mtakuja niuwa kwa jinaya hii ambayo sikuukusudia. Mola wangu Mlezi akanitunukia fahamu na ilimu, kwa fadhila zake na neema zake, na akanifanya mmoja katika Mitume.

22 Musa akaashiria sifa katika sifa ova kabisa za Firauni, nayo ni kuwa kawafanya watumwa Wana wa Israili, na akiwauwa watoto wao wanaume. Na akakataa kukuita kule kulelewa kwake katika jumba la Firauni kuwa ni neema, kwani yaliyo sabibisha hayo ni yale aliyo kwisha yataja, ndio yeye alitupwa mtoni aokoze asiuliwe. Akaishia kwenye jumba la Firauni. Na lau kuwa si hivyo basi angeli lelewa na wazazi wake.

23 Firauni akasema: Na nini hizo sifa za Mola Mlezi wa walimwengu wote ambaye unakithiri kumtaja, na wewe unadai kuwa ni Mtume wake, na hali sisi hatujui lolote khabari zake?

24 Musa akasema: Yeye huyo ndiye Mwenye kuzimiliki mbingu na ardhi na kila kilio baina yao. Ikiwa nyinyi mna yakini ya ukweli wa jawabu hii basi mtanafika, na mtaongoka, na mtajua kuwa ufalme wa Firauni wa kujidai haufui dafu mbele ya Ufalme wake Mwenyezi Mungu. Kwani ufalme wa Firauni haupindukii hata eneo moja katika hii dunia.

25 Firauni kuonyesha mastaajabu kwa wale walio mzunguka kwa kuwa Musa katika jawabu yake alipo mtaja Mola wake Mlezi na akadhukuru Ufalme wake hakuugusia hata kidogo ufalme wa Firauni, alisema: Mwayasikiaje maneno ya Musa?

26 Musa akiendelea na usemi wake bila ya kujali hasira za Firauni na uchafu wa maneno yake, akasema: Ndiye huyo Mola Mlezi wa walimwengu wote, aliye kuumbeni nyinyi na baba zenu walio tangulia. Na miongoni mwa hao walikuwako walio dai ungu kama unavyo dai wewe. Na wao wameteketee. Na wewe utateketea, na hayo unayo yadai yatapotelea mbali. Kwani Mungu wa kweli hafi.

27 Firauni akwaambia watu wake yale yanayo mtibuwa roho na kumghadhibisha, akautaja Utume wa Musa ni kwao wao, wala si kwake yeye, na akambandikiza wazimu, kwa kuwa ati akiulizwa kitu hujibu kingine, na anamsifu Mola Mlezi kwa sifa za kiajabu ajabu. Na kwa hivyo Firauni anawahimiza wamkadhibishe.

28 Musa akasema: Ikiwa nyinyi mna akili, basi uaminini Ujumbe wangu. Kwani kuchomoza jua na kuchwa kwake kwa mpango madhubuti ni dalili wazi ya Mwenye kuumba. Kwa hivyo basi ni nyinyi ndio mnastahiki kuambiwa wendawazimu.

29 Firauni akamwambia Musa: Ukimfuata mungu yeyote badala yangu mimi, utakuwa mmoja katika wanao ijua hali yao mbaya katika magereza yangu. Na yeye Firauni kaangukia kitisho hichi baada ya kushindwa kuondoa athari za kazi za Muumbaji.

30 Musa akasema kwa upole kwa kutumai asaa akaamini: Utanitia gerezani hata nikikuletea ushahidi mkubwa wa ukweli wa haya niyasemayo?

31. Akasema: Kilete basi, kama wewe ni katika wasemao kweli.³¹
32. Basi akaitupa fimbo yake, mara ikawa nyoka wa kuonekana dhaahiri.³²
33. Na akautoa mkono wake, na mara ukawa mweupe kwa watazamao.³³
34. (Firauni) akawaambia waheshimiwa walio mzunguka: Hakika huyu ni mchawi mtaalamu.³⁴
35. Anataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake. Basi mna shauri gani?³⁵
36. Wakasema: Mpe muda yeye na nduguye na uwatume mijini wapigao mbiu ya mgambo.³⁶
37. Wakuletee kila mchawi bingwa mtaalamu.³⁷
38. Basi wakakusanywa wachawi wakati na siku maalumu.³⁸
39. Na watu wakaambiwa: Je! Mtakusanyika?³⁹
40. Huenda tutawafuata wachawi wakiwa wao ndio watakao shinda.⁴⁰
41. Basi walipo kuja wachawi wakamwambia Firauni: Je! Tutapata ujira tukiwa sisi ndio tulio shinda?⁴¹
42. Naam! Na hakika mtakuwa katika watu wa mbele.⁴²
43. Musa akwaambia: Tupeni mnavyo taka kutupa.⁴³
44. Basi wakatupa kamba zao na fimbo zao, na wakasema: Kwa nguvu za Firauni hakika sisi hapana shaka ni wenye kushinda.⁴⁴
45. Musa tena akatupa fimbo yake, nayo mara ikavimeza walivyo vizua.⁴⁵

31 Firauni akasema: Ulete ushahidi utao onyesha Unabii wako kama wewe kweli unasema kweli katika wito wako. Kasema hayo kwa tamaa ya kuwa huenda akapata kipengee cha udhaifu katika hoja zake.

32 Musa akaitupa fimbo yake mbele yao. Ikageuka nyoka kweli kweli, si kitu cha uwongo cha uchawi kinacho fanana na nyoka.

33 Musa akautoa mkono wake kutoka mfukoni mwake. Hiyo ni Ishara ya pili. Nao ukawa mweupe, bila ya maradhi, hata wakashangaa watazamaji kwa kumetuka kwake.

34 Firauni akawaambia watu wake: Hakika Musa ni mchawi bingwa katika uchawi wake. Kasema hayo kwa kuchelea watu wake wasiifuate Haki waliyo iona kwa Musa.

35 Tena Firauni akasema: Mchawi huyu anataka kunifanyia kahari apate kukutoeni katika hii nchi yenu. Na haya ni uchochezi dhidi ya Musa, kwani katika la dhiki mno katika hayo yaliyo dhiki ni mtu kuiacha nchi yake, na khasa ikiwa kwa kahari. Naye akataka mawazo ya wale walio kuwa wanamuabudu. Kasahau ungu wake kwa nguvu za Ishara za Musa.

36 Watu wake wakamwambia: Akhirisha kukata shauri yao hawa, na uwatume askari wende wawakusanye wachawi katika raia zako. Kwani uchawi hupingwa kwa uchawi.

37 Watakuletea wengi, na wote wameboba kwa uchawi, na wamemshinda Musa kwa ufundi na ustadi. Wamekusudia kwa haya kumpunguzia dukuduku lake Firauni.

38 Wakakusanywa wachawi kutoka kila upande wa nchi. Wakawekewa wakati wa mchana siku ya Sikukuu kukutana na Musa.

39 Na watu wakahimizana kuhudhuria siku hiyo waone ramsa wakiambizana: Mtakusanyika? Yaani ndio: Mkusanyike!

40 Wakatangaza matarajio yao ya kushinda wachawi, ili wapate kuthibiti katika dini yao, na pia ndio kampeni ya nguvu na juhudi apate kushindwa Musa.

41 Walipo kuja wachawi kwa Firauni walimwambia: Je! Tutapata kwako ujira mkubwa pindi tukishinda?

42 Firauni akasema: Naam, mtapata mnacho kisema. Na juu ya huo ujira mkubwa mtakuwa watu wa karibu kwangu, watu wa cheo na madaraka.

43 Ulipo fika wakati ulio wekwa katika siku iliyo pangwa Musa aliwaambia wachawi: Tupeni huo uchawi mnao taka kuutupa.

44 Wakazitupa kamba zao na fimbo zao, na watu wakazugwa wakaona kama ni nyoka wanakwenda. Wakaapa kwa utukufu wa Firauni na nguvu zake hapana shaka hawa leo watashinda.

45 Musa tena akatupa fimbo yake. Mara ikawa joka kubwa likaingia kuvimeza vile walivyo vizua kwa uchawi, navyo ni kamba na fimbo, wakidanganya kuwa ni nyoka wanao kwenda.

46. Hapo wachawi walipinduka wakasujudu.⁴⁶
47. Wakasema: Tunamuamini Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁴⁷
48. Mola Mlezi wa Musa na Harun.⁴⁸
49. (Firauni) akasema: Je! Mmemuamini kabla sijakuruhusuni? Bila ya shaka yeye basi ndiye mkubwa wenu aliye kufunzeni uchawi. Basi mtakuja jua! Nitakata mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakubandikeni misalabani nyote.⁴⁹
50. Wakasema: Haidhuru, kwani sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi.⁵⁰
51. Hakika sisi tunatumai Mola wetu Mlezi atatusamehe makosa yetu, kwa kuwa ndio wa kwanza wa kuamini.⁵¹
52. Na tulimuamrisha Musa kwa wahyi: Nenda na waja wangu wakati wa usiku. Kwa hakika mtafuatwa.⁵²
53. Basi Firauni akawatuma mijini wapiga mbiu za mgambo.⁵³
54. (Wakieneza): Hakika hawa ni kikundi kidogo.⁵⁴
55. Nao wanatuudhi.⁵⁵
56. Na sisi ni wengi, wenye kuchukua hadhari.⁵⁶
57. Basi tukawatoa katika mabustani na chemchem,⁵⁷
58. Na makhazina, na vyeo vya hishima,⁵⁸
59. Kadhaalika; na tukawarithisha hayo Wana wa Israili.⁵⁹

46 Wachawi wakaanguka wakasujudu kumsujudia Mwenyezi Mungu, walipo yakinika kuwa mambo ya Musa si uchawi.

47 Wakasema ili kutia mkazo kule kusujudu kwao kwa kauli yao: Tunamuamini Mola Mlezi wa walimwengu wote.

48 Na wakabainisha kuwa hakika Mola Mlezi wa walimwengu wote walio muamini ndiye: Mola Mlezi wa Musa na Harun.

49 Firauni kwa kukasarika kuwa wale wachawi wamemuamini Musa bila ya yeye kuwapa ruhusa, aliwatishia ya kwamba yeye ndiye mwalimu wao aliye wafunza fani za uchawi, na watakuja jua adhabu itakayo wateremkia. Akawaambia: Nitakata mikono yenu na miguu yenu mbali mbali, nitakata wa kulia huu kwa wa kushoto huu, na kinyume cha hayo. Na nyote nitakutundikeni juu ya misalaba.

50 Wachawi wakasema: Hapana la kutudhuru sisi kwa adhabu unazo tutishia, kwani sisi ni wenye kurejea kwenye malipo ya Mola wetu Mlezi. Na Yeye ndiye mbora wa kulipa na mbora wa kuadhibu.

51 Hakika sisi tunataraji Mola wetu Mlezi atatusamehe makosa yetu tuliyo yafanya zamani, kwa kuwa sisi ndio wa mwanzo wa Waumini katika kaumu yako.

52 Na Mwenyezi Mungu alimpa wahyi Musa a.s. atoke usiku usiku pamoja na Waumini miongoni mwa Wana wa Israili, ilipo kuwa tena haiwi kumsubirisha Musa. Mpango ukawa wa makundi mawili kwamba atangulie Musa na kaumu yake, na Firauni afuatie na kaumu yake, mpaka waingie katika maingilio ya njia ya baharini, na Mwenyezi Mungu awateketeze.

53 Firauni akawatuma askari wake katika miji ya mamlaka yake, wawakusanye wenye maguvu katika kaumu yake, alipo jua kuwa Musa kesho toka na Wana wa Israili, ili awazuie lile walilo kusudia.

54 Firauni akasema: Hakika hawa Wana wa Israili walio kimbia na Musa ni taifa dogo kwa nguvu zao. Idadi yao ni chache. Anasema hayo kutia mori katika nyoyo za askari wake.

55 Na wao juu ya hivyo, wanatutibua roho kwa kuvunja amri yetu na kutoka bila ya idhini yet.

56 Na sisi ni wengi. Miongoni mwa ada zetu ni kuchukua hadhari, na kuwa macho, na kupania.

57 Tukawatoa Firauni na askari wake kwenye nchi yao iliyo fanana na mabustani yapitiwayo na mito kati yao, wakaangamia kwa kujitenga kwao na Haki, na kuchochewa kutaka kumfuatia Musa, kama ilivyo kuja katika Aya tatu zilizo tangulia

58 Tukawatoa, kadhaalika, kwenye khazina za dhahabu na fedha, na majumba waliyo kuwa wakiyakalia, wakineemeka kwa uzuri wake na ubora wa starehe zake.

59 Ni kutoka kama huku kwa ajabu tulivyo kueleza ndivyo tulivyo watoa, na tukawapa ufalme huo na kila namna ya neema zilizo kuwamo Wana wa Israili, baada ya kuwa masikini hawana mbele wala nyuma.

60. Basi wakawafuata lilipo chomoza jua.⁶⁰
61. Na yalipo onana majeshi mawili haya, watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana!⁶¹
62. (Musa) akasema: Hasha! Hakika yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa!⁶²
63. Tulimletea wahyi Musa tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa.⁶³
64. Na tukawajongeza hapo wale wengine.⁶⁴
65. Tukawaokoa Musa na walio kuwa pamoja naye wote.⁶⁵
66. Kisha tukawazamisha hao wengine.⁶⁶
67. Hakika bila ya shaka katika hayo ipo Ishara; lakini wengi wao si katika wenye kuamini.⁶⁷
68. Na kwa hakika Mola wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.⁶⁸
69. Na wasomee khabari za Ibrahim.⁶⁹
70. Alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Mnaabudu nini?⁷⁰
71. Wakasema: Tunaabudu masanamu, daima tunayanyenyekea.⁷¹
72. Akasema: Je! Yanakusikieni mnapo yaita?⁷²
73. Au yanakufaeni, au yanakudhuruni?⁷³
74. Wakasema: Bali tumewakuta baba zetu wakifanya hivyo hivyo.⁷⁴

60 Firauni na watu wake wakakaza mwendo ili wapate kuwawahi Wana wa Israili. Wakawakuta wakati wa kuchomoza jua.

61 Walipo onana makundi mawili, watu wa Musa walisema: Hakika Firauni na watu wake watatupata. Basi tutaangamia.

62 Musa akasema: Hakika mimi ninao uangalizi wa Mwenyezi Mungu unao nifuata kwa kunihifadhi. Na Yeye ataniongoza kwenye Njia ya uwokovu. Amesema hayo ili awatuze kuwa watasalimika, na iwe mbali na mawazo yao fikra ya kutisha kwamba watakuja patikana.

63 Tukamuamrisha Musa kwa wahyi, ufunuo, aipige bahari kwa fimbo yake. Ikapasuka bahari njia kumi na mbili kwa mujibu wa idadi ya mataifa ya Wana wa Israili. Kila njia katika hizo njia ilikuwa na kizuizi cha maji yaliyo nyanyuka kama mlima ulio simama imara.

64 Tukawajongeza Firauni na kaumu yake mpaka wakaingia kwenye zile njia nyuma ya Musa na kaumu yake.

65 Tukamwokoia Musa na walio kuwa pamoja naye kwa hifadhi ya bahari nayo imeshikamana, mpaka wakamalizika kuvuka.

66 Kisha tukamzamisha Firauni pamoja na walio kuwa pamoja naye kwa kuwafudikiza kwa maji pale walipo wafuata.

67 Hakika katika vituko hivi vya ajabu vya kiungu pana funzo la kuzingatia kwa atakaye kunafika. Lakini watu wengi si wenye kusadiki.

68 Hakika Muumba wako na Mlezi wako ndiye huyo Mwenye nguvu katika kuwaadhibu wanao kanusha, Mwenye kuwaneemesha kwa rehema Waumini.

69 Ewe Mtume! Na wasomee makafiri hadithi ya Ibrahim, *Alayhi Ssalaam*.

70 Alipo mwambia baba yake: Mnaabudu kitu gani hichi, ambacho hakifai kuabudiwa? Anakusudia kwa hayo kuyakebehi masanamu.

71 Wakasema kujibu kwa njia ya kujitapa: Tunaabudu masanamu, nasi tunadumu daima dawamu tukiyaabudu, kwa kuyaadhimisha na kuyatukuza!

72 Ibrahim akasema: Kwani yanasikia madua yenu? Au yanakuitikieni mnapo yaomba? Kwa hayo anakusudia kuwanabihisha upotovu wa mwendo wao.

73 Au yanakuleteeni manufaa mnapo yat'ii? Au yanakupatilizeni kwa madhara mkiyaasi?

74 Wakasema: Hawafanyi lolote katika hayo. Lakini sisi tumewakuta baba zetu wakiyaabudu mfano wa ibada yetu. Basi sisi tukawafwata kwa waliyo kuwa wakiyafanya.

75. Je! Mmewaona hawa mnao waabudu-⁷⁵
76. Nyinyi na baba zenu wa zamani?⁷⁶
77. Kwani hakika hao ni adui zangu, isipo kuwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁷⁷
78. Ambaye ndiye aliye niumba, na Yeye ndiye ananiongoa,⁷⁸
79. Na ambaye ndiye ananilisha na kuninyweshwa.⁷⁹
80. Na ninapo ugua ni Yeye ndiye anaye niponesha.⁸⁰
81. Na ambaye atanifisha, na kisha atanihuisha.⁸¹
82. Na ambaye ndiye ninaye mtumai kunisamehe makosa yangu Siku ya Malipo.⁸²
83. Mola wangu Mlezi! Nitunukie hukumu na uniunganishe na watendao mema.⁸³
84. Na unijaalie nitajwe kwa wema na watu watakao kuja baadaye.⁸⁴
85. Na unijaalie katika warithi wa Bustani za neema.⁸⁵
86. Na umsamehe baba yangu, kwani hakika alikuwa miongoni mwa wapotovu.⁸⁶
87. Wala usinihizi Siku watapo fufuliwa.⁸⁷
88. Siku ambayo kwamba mali hayato faa kitu wala wana.⁸⁸
89. Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi.⁸⁹
90. Na Pepo itasogezwa kwa wachamngu.⁹⁰

75 Ibrahim akasema kwa kuwasusuika: Je! Mlifikiri hata mkalijua jambo lolote lililo kupelekeeni kudumu na kuyaabudu hayo masanamu?

76 Nyinyi na baba zenu wa zamani - ati haya yanastahiki kuabudiwa au la? Lau mngeli zingatia mngeli jua kuwa hakika nyinyi mko katika upotovu ulio wazi.

77 Kwani hakika hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni maaadui kwangu mimi na kwenu. Basi mimi siwaabudu hao. Lakini ninaye muabudu na najijongeza kwake ni Muumba wa walimwengu wote, na Mwenye kumiliki mambo yao, na Mwenye kuwalinda.

78 Ambae ndiye aliye nizua kabla sijawa chochote akaniumba kwa bora ya umbo, na akanitunukia uwongofu wa kunifikishia kwenye mafanikio yangu ya duniani na Akhera.

79 Na Yeye ndiye aliye nineemesha kwa vyakula na vinywaji, na akaniwezesha kuvipata na kunafiika kwavyo, ili kuhifadhi uhai wangu.

80 Na yakinishukia maradhi ni Yeye ndiye anaye niponesha, kwa kunisahilishia sababu za kupona na kuniwezesha kuzipata.

81 Na Yeye ndiye atanifisha ikifika ajali yangu, na tena atanihuisha mara nyengine kwa ajili ya hisabu na malipo.

82 Na Yeye ndiye ninaye mtumai kunighufiria na kuyasemehe makosa yangu madogo madogo ya kujikwaa duniani, utapo fika wakati wa hisabu.

83 Ibrahim a.s. akasema kwa kuomba: Mola wangu Mlezi! Nitunukie ukamilifu wa ilimu na vitendo, ili nipate kustahili kuubeba Ujumbe wako na hukumu kwa waja wako, na niwezeshe niungane pamoja na kundi la watendao wema.

84 Na nijaalie nipate sifa nzuri na kumbusho jema kwa kaumu zitazo kuja baada yangu, mabaki yake yasalie mpaka Siku ya Kiyama.

85 Na nijaalie katika waja wako ulio watunukia neema za Peponi, kuwa ni malipo kwa sababu ya Imani yao kukuamini Wewe, na ibada yao kukuabudu Wewe.

86 Na mjaalie baba yangu astahili msamaha kwa kumwezesha kuwa Muislamu. Na yeye alikuwa kamuahidi kusilimu siku alio achana naye, kwani yeye huyo baba alikuwa ameitupa kando njia ya uwongofu na uwongozi.

87 Wala usinitie aibu au hizaya mbele ya watu, Siku watapo tolewa makaburini kwa ajili ya hisabu na malipo.

88 Siku ambayo hapana mtu ataye nafiika kwa mali ayatoe, au kwa wana wamsaidie.

89 Isipo kuwa aliye kuwa Muumini, na akamkabili Mwenyezi Mungu na moyo ulio mzima, hauna maradhi ya ukafiri, na unaafiki, na riya (kujionesha).

90 Na Pepo itajongezwa, na itakaribishwa pahala pa watu wema. Basi wataiendea wale walio jikinga na ukafiri na maasi, na wakaikubali Imani na ut'iifu duniani.

91. Na Jahannamu itadhihirishwa kwa wapotovu.⁹¹
92. Na wataambiwa: Wako wapi mlio kuwa mkiwaabudu?⁹²
93. Badala ya Mwenyezi Mungu? Je! Wanakusaidieni, au wanajisaidia wenyewe?⁹³
94. Basi watawaturumizwa humo wao na hao wakosefu,⁹⁴
95. Na majeshi ya Ibilisi yote.⁹⁵
96. Watasema, na hali ya kuwa wanazozana humo:⁹⁶
97. Wallahi! Kwa yakini tulikuwa katika upotovu ulio dhaahiri,⁹⁷
98. Tulipo kufanyeni ni sawa na Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁹⁸
99. Na hawakutupoteza ila wale wakosefu.⁹⁹
100. Basi hatuna waombezi.¹⁰⁰
101. Wala rafiki wa dhati.¹⁰¹
102. Laiti tungeli pata kurejea tena tungeli kuwa katika Waumini.¹⁰²
103. Hakika katika haya ipo Ishara, lakini wengi wao hawakuwa wenye kuamini.¹⁰³
104. Na hakika Mola wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.¹⁰⁴
105. Kaumu ya Nuhu waliwakadhibisha Mitume.¹⁰⁵
106. Alipo waambia ndugu yao, Nuhu: Je! Hamchimngu?¹⁰⁶
107. Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.¹⁰⁷

91 Na Moto utaletwa mbele ya walio iacha Dini ya Haki, mpaka ndimi zake zikaribie kuwanyakua, nao watakuwa majutoni.

92 Wakaambiwa kwa kuwatahayarisha: Iko wapi hiyo miungu yenu mliyo kuwa mkiiabudu badala ya Mwenyezi Mungu?

93 Badala ya Mwenyezi Mungu, na mnadai kuwa ati ndio itakuombeeni hii leo? Je! Inakufaeni kitu kwa kukunusuruni, au hata inajifaa wenyewe kujisaidia? Hapana lolote. Kwani wao na miungu yao ni kuni za Moto.

94 Watatumbukizwa katika Jahannamu kifudufudi, wakipinduliwa pinduliwa mpaka waishie ndani kabisa shimoni, wao na walio wapoteza na wakawatia katika madhambi na upotovu.

95 Na pamoja nao watakuwapo wasaidizi wa Ibilisi walio kuwa wakiwapambia shari na madhambi, au wale watu na majini walio wakiwafuata katika maasi.

96 Watasema huku wakiungama makosa yao, na huku wanagombana na miungu yao waliyo kuwa wakiabudu:

97 Wallahi! Hakika sisi tulikuwa katika dunia yetu tumepotea kweli, na wajinga wa kutupwa, na tumeiacha Haki ambayo haina kificho ndani yake.

98 Pale tulipo kufanyeni nyinyi tulio kuabuduni badala ya Mwenyezi Mungu kuwa ati ni sawa sawa na Mola Mlezi wa walimwengu wote katika kustahiki kuabudiwa, juu ya kuwa hamjiwezi wala hamfai kwa lolote.

99 Wala hapana walio tutia katika hilaki hii ila wakosefu walio tupotoa tukaiwacha Njia Iliyo Nyooka.

100 Basi hapana wa kuombwa akaja kutuvua na adhabu hii kama tulivyo dhania pale kwanza.

101 Wala hapana rafiki wa kuwaonea uchungu kwa hali yao, licha ya kuwaokoa.

102 Basi hapo ndio wanajitamania nafsi zao lau wangeli rejea duniani wapate kuwa Waumini ili waokoke.

103 Na hakika katika khabari za Ibrahim zilizo tajwa yapo mawaidha na mazingatio kwa mwenye kutaka mawaidha na akazingatia. Na wala si wengi katika watu wako wanao somewa khabari hizi wenye kuitikia wito wako.

104 Na hakika hapana shaka Mola wako Mlezi ni Muweza wa kuwaadhibu wanao kadhibisha, naye ni Mfadhili wa watu wema kwa neema nyingi.

105 Na Mwenyezi Mungu ametaja khabari za Nuhu kwa kauli yake: Kaumu ya Nuhu iliukanusha Utume wake, wakamrudishia mwenyewe. Kwa kitendo hicho ikawa wamewakadhibisha Mitume wote wa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa wito wao ni mmoja katika asli yake na lengo lake.

106 Waliukanusha Utume huu pale alipo waambia ndugu yao Nuhu - ndugu kwa makhusiano ya nasaba si kwa Dini - akiwahadharisha: Hamumchi Mwenyezi Mungu, mkaacha kuabudu wenginewe?

107 Hakika mimi ni Mtume, nimetumwa kwenu nikuongoeni kwenye Njia ya wongofu, na ni muaminifu

- 108.** Basi Mcheni Mwenyezi Mungu, na nit'iini mimi.¹⁰⁸
109. Na sikutakini juu yake ujira, kwani ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹⁰⁹
110. Basi Mcheni Mwenyezi Mungu, na nit'iini mimi.¹¹⁰
111. Wakasema: Je! Tukuamini wewe, hali wanao kufuata ni watu wa chini?¹¹¹
112. Akasema: Nayajuaje waliyo kuwa wakiyafanya?¹¹²
113. Hisabu yao haiko ila kwa Mola wao Mlezi, laiti mngeli tambua!¹¹³
114. Wala mimi si wa kuwafukuza Waumini.¹¹⁴
115. Mimi si cho chote ila ni Mwonyaji wa dhaahiri shaahiri.¹¹⁵
116. Wakasema: Ikiwa huachi, ewe Nuhu, bila ya shaka utapigwa mawe.¹¹⁶
117. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikanusha.¹¹⁷
118. Basi hukumu baina yangu na wao kwa hukumu yako, na uniokoe mimi na walio pamoja nami, Waumini.¹¹⁸
119. Kwa hivyo tukamwoko a yeye na walio kuwa pamoja naye katika marikebu iliyo sheheni.¹¹⁹
120. Kisha tukawazamisha baadaye walio bakia.¹²⁰
121. Hakika katika haya ipo Ishara, lakini si wengi wao walio kuwa Waumini.¹²¹
122. Na hakika Mola wako Mlezi ndiye Yeye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.¹²²

wa kufikisha huu Ujumbe.

108 Basi mkhofuni Mwenyezi Mungu, na fuateni amri yangu katika hayo ninayo kuitieni kwayo ya kumuamini Mwenyezi Mungu wa pekee na kumt'iini.

109 Na wala sitaki kwenu ujira kwa ajili ya ninayo kupeni ya nasaha na wito. Na sina malipo ila kwa Mwenye kuwaumba viumbe wote, Aliye miliki mambo yao.

110 Basi tahadarini na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na fuateni ninayo kuamrisheni.

111 . Watu wa Nuhu, huku wakiukataa wito wake, walisema: Hatutokuwa na imani nawe maadamu wanakufuata watu duni kabisa, wasio kuwa na hadhi wala mali.

112 Nuhu akasema: Kitu gani cha kunijuvya uchache wa hadhi yao na mali yao? Nikitakacho mimi kwao ni Imani yao bila ya kutafuta kuzijua kazi zao.

113 Hapana wa kuwalipa kwa vitendo vyao na kazi zao ila Mola wangu Mlezi; kwani Yeye ndiye anaye yajua vyema ya undani wao. Kama nyinyi ni watu watambuzi mngeli tambua hayo.

114 Wala mimi siye wa kuwafukuza watu wanao uamini wito wangu vyovyote itavyo kuwa hali yao ya ufakiri au utajiri, kwa sababu ati ya kukubaliani nyinyi kwa mtakalo ili ndio mpate kuniamini.

115 Mimi si chochote ila ni Mtume niliye toka kwa Mwenyezi Mungu kuwaonya walio wajibikiwa kwa onyo lililo wazi, kwa ushahidi wa kutenganisha baina ya kweli na uwongo, bila ya farka yoyote baina ya mtukufu na mnyonge. Basi vipi itanifalia mimi kuwafukuza Waumini kwa sababu ya ufakiri wao?

116 Wakasema: Ewe Nuhu! Ikiwa hutoacha huu wito wako basi jua yakini tutakupopoa mawe. Yaani wanakusudia kwa haya kumtishia kumuwa.

117 Nuhu kuonyesha kushikilia watu wake kuukadhibisha wito wake, alisema: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikanusha! Kuthibitisha kuwa wanastahiki maafizo yake.

118 Basi tuhukumie baina yangu na wao, kwa hukumu ya kuwaangamiza wanao pinga Upweke wako, na wakamkadhibisha Mtume wako! Na niokoe mimi na Waumini walio pamoja nami na adhabu ya uasi wao.

119 Ndio hivyo tukamwoko a yeye pamoja na walio amini katika safina iliyo pakia pomoni wao hao pamoja na mahitaji yao, kwa kuitikia dua yake.

120 Baada ya kuokoka kwa Nuhu na walio amini, Mwenyezi Mungu aliwazamisha walio baki katika kaumu ya Nuhu walio kuwa hawakuamini.

121 Hakika katika yaliyo simuliwa na Qur'ani juu ya khabari za Nuhu ni hoja ya kuthibitisha ukweli wa Mitume na uwezo wa Mwenyezi Mungu. Na katika watu walio somewa hadithi hizi si wengi walio amini.

122 Na hakika Mola wako Mlezi ndiye Yeye Mwenye nguvu za kumuadhibu kila jabari mwenye inda, Mwenye kuwaneemesha wachamngu kwa kila namna ya fadhila.

123. Kina A'd waliwakanusha Mitume.¹²³
124. Alipo waambia ndugu yao, Hud: Je! Hamchimngu?¹²⁴
125. Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.¹²⁵
126. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, na nit'iini mimi.¹²⁶
127. Wala sikutakeni juu yake ujira, kwani ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹²⁷
128. Je! Mnajenga juu ya kila mnyanyuko kumbusho la kufanyia upuuzi?¹²⁸
129. Na mnajenga majengo ya fakhari kama kwamba mtaishi milele!¹²⁹
130. Na mnapo tumia nguvu mnatumia nguvu kwa ujabari.¹³⁰
131. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, na nit'iini.¹³¹
132. Na mcheni aliye kupeni haya mnayo yajua.¹³²
133. Amekupeni wanyama wa kufuga na wana.¹³³
134. Na mabustani na chemchem.¹³⁴
135. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku Kubwa.¹³⁵
136. Wakasema: Ni mamoja kwetu, ukitupa mawaidha au hukuwa miongoni mwa watoao mawaidha.¹³⁶
137. Haya si chochote ila ni mtindo wa watu wa tokea zamani.¹³⁷

123 Kabila ya A'di ilimkanusha Mtume wao Hud a.s. Na kwa hivyo wakawa ndio wamewakadhibisha Mitume wote, kwa kuwa wito wao ni mmoja katika asli yake na lengo lake.

124 Alipo waambia ndugu yao Hud: Hamumwogopi Mwenyezi Mungu, mkamsafia ibada?

125 Hakika mimi nimetumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ili nikuongoeni mfuata uwongozi, na ni mwenye kuulinda ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Naufikisha ujumbe huo kama alivyo niamrisha Mola wangu Mlez.

126 Basi ifuateni amri ya Mwenyezi Mungu. Na ikhofuni adhabu yake. Na t'iini ninayo kuamrisheni yanayo toka kwa Mwenyezi Mungu.

127 Wala kwa hii nasaha yangu na uwongozi wangu sitaki kwenu ujira. Sina malipo isipo kuwa kwa Muumba wa viumbe vyote.

128 Je! Mnasimamisha juu ya kila pahala palipo nyanyuka katika nchi jengo refu kwa ajili ya kujifakhirisha, na mnakutana humo kwa mambo ya upuuzi na fisadi? Mwenyezi Mungu *Subhanahu* anataka kwa haya kuwazindua watende yatakayo wanufaisha, na anawataharisha kwa kuacha kwao Imani na vitendo vyema.

129 Na mnajenga majumba ya fakhari na imara, na mahodhi ya maji, kwa kutaraji kuishi milele katika dunia hii, kama kwamba hamtakufa.

130 Na mnapo ingia kutesa, mnapita kiasi katika uasi na uvamizi wa jeuri, mnauwa, na mnapiga kwa chuki bila ya huruma.

131 Mwogopeni Mwenyezi Mungu katika kutumia nguvu, Na fuateni amri yangu katika ninayo kuitieni. Kwani hayo hakika ndiyo yatakayo kukufaeni na ndiyo yatakayo dumu zaidi.

132 Na tahadharini na ghadhabu za Mwenyezi Mungu aliye kukunjulieni neema zake, kwa mnayo yajua yaliyo mbele yenu ya vipawa vyake vya namna mbali mbali.

133 Kama alivyo kupeni mifugo kama ngamia, na ng'ombe, na kondoo, na mbuzi, na wana wenye nguvu, wakukulindieni mifugo yenu, na kukusaidieni katika shida za maisha.

134 Na mabustani yenye matunda, na chemchem zenye kutiririka maji mnayo yahitajia.

135 Mimi nina khofu asije Mwenyezi Mungu akakuteremshieni adhabu kali hapa duniani, na Akhera akakutieni katika Moto wa Jahannamu kwa sababu ya ujabari wenu na starehe alizo kustarehesheni Mwenyezi Mungu.

136 Wakasema kwa kumkejeli: Ni sawa kwetu, ukitupa waadhi na kutuonya au ukawa si katika wenye kutoa waadhi.

137 Haya uliyo tuletea si lolote ila ni uwongo na upotovu wa watu wa zamani. Wao wamezoea kuzua kama hivyo. Kwa hivyo sisi hatutaacha tuliyo kuwa nayo.

138. Wala sisi hatutaadhibiwa.¹³⁸
139. Wakamkanusha; nasi tukawaangamiza. Hakika bila ya shaka katika haya ipo Ishara. Lakini hawakuwa wengi wao wenye kuamini.¹³⁹
140. Na hakika Mola wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.¹⁴⁰
141. Kina Thamud waliwakanusha Mitume.¹⁴¹
142. Alipo waambia ndugu yao Saleh: Je! Hamumchimngu?¹⁴²
143. Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.¹⁴³
144. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, na nit'iini.¹⁴⁴
145. Wala sikutakini ujira juu yake. Ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹⁴⁵
146. Je! Mtaachwa salama usalimina katika haya yaliyopo hapa?¹⁴⁶
147. Katika mabustani, na chemchem?¹⁴⁷
148. Na konde na mitende yenye makole yaliyo wiva.¹⁴⁸
149. Na mnachonga milimani majumba kwa ustadi.¹⁴⁹
150. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, na nit'iini mimi.¹⁵⁰
151. Wala msit'ii amri za walio pindukia mipaka,¹⁵¹
152. Ambao wanafanya ufisadi katika nchi, wala hawatengenezi.¹⁵²
153. Wakasema: Hakika wewe ni miongoni mwa walio rogwa.¹⁵³
154. Wewe si chochote ila ni mtu kama sisi. Basi lete Ishara ukiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.¹⁵⁴

138 Wala sisi hatutaadhibiwa kwa vitendo tuvitendavyo.

139 Basi wakaendelea kushikilia kumkanusha. Mwenyezi Mungu akawafanyia haraka kuwateketeza. Hakika katika hayo alipo wateremshia Mwenyezi Mungu kina A'di kwa kuwa ni malipo kwa ukanushi wao, ni hoja inayo juulisha ukamilifu wa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Na si wengi katika wanao somewa khabari za A'adi walio Waumini.

140 Na Mola wako Mlezi ndiye Mtenda nguvu wa kuwashinda hao majabari, Mwenye kuwarehemu Waumini.

141 Kabila ya Thamud ilimkanusha Saleh katika Ujumbe wake na wito wake, na kwa hivyo ikawa wamewakanusha Mitume wote, kwa kuwa asli ya Ujumbe ni moja, na lengo ni moja.

142 Ewe Mtume! Watajia watu wako, wakati ule kina Thamud walipo ambiwa na ndugu yao kwa uzao na uwananchi, si kwa dini, Saleh: Hamumwogopi Mwenyezi Mungu, mkamuabudu Yeye tu?

143 Hakika mimi nimetumwa na Mwenyezi Mungu kwenu kwa mambo yenye kheri yenu na mafanikio yenu. Na mimi ni mwenye kuuhiifadhi Ujumbe huu kama nilivyo upokea kwa Mwenyezi Mungu.

144 Kwa hivyo tahadharini na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na nifuatani kwa haya ninayo kuitieni kwayo kutokana na amri zake.

145 Wala sitaki kwenu ujira wowote kwa hii nasaha yangu na uwongozi wangu. Ujira wangu uko kwa Mwenye kumiliki walimwengu wote.

146 Lilio wazuia ni kule kuamini kwao kwamba ati wataselelea katika zile starehe, watasalimika na adhabu, na kutoweka, na maut,

147 Katika mabustani ya matunda, na chemchem zenye kutoa maji matamu,

148 Na konde zilizo wiva, na mitende ambayo mazao yake yamedhihiri mapevu na laini.

149 Na mnachonga milimani majumba kwa ufundi na ustadi katika hayo mnayo yaunda.

150 Basi iogopeni adhabu ya Mwenyezi Mungu, kwa kuto mshukuru kwenu kwa neema zake; na pokeeni nasiha yangu na muitende.

151 Wala msiit'ii amri ya walio pindukia mipaka kwa ushirikina na kufuata pumbao na matamano.

152 Ambao wanapitisha maisha yao katika ardhi kwa uharibifu, wala hawafanyi ya maslaha ya kutengeneza nchi.

153 Wakasema: Wewe si chochote isipo kuwa miongoni mwa walio rogwa kikweli mpaka zikapotea akili zao. Na katika jawabu hii mna ukali na usafihi.

154 Wewe si chochote ila ni mmoja unaye fanana na sisi kwa ubinaadamu, basi yawaje uwe bora kuliko

- 155.** Akasema: Huyu ngamia jike; awe na zamu yake ya kunywa, na nyinyi muwe na zamu yenu ya kunywa katika siku maalumu.¹⁵⁵
- 156.** Wala msinguse kwa uwovu, isije ikakushikeni adhabu ya Siku Kubwa.¹⁵⁶
- 157.** Lakini wakamuwa, na wakawa wenye kujuta.¹⁵⁷
- 158.** Basi ikawapata adhabu. Hakika katika hayo ipo Ishara. Lakini hawakuwa wengi wao wenye kuamini.¹⁵⁸
- 159.** Na hakika Mola wako Mlezi ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.¹⁵⁹
- 160.** Watu wa Lut'i waliwakanusha Mitume.¹⁶⁰
- 161.** Alipo waambia ndugu yao, Lut'i: Je! Hamumchimngu?¹⁶¹
- 162.** Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu kwenu.¹⁶²
- 163.** Basi mcheni Mwenyezi Mungu na nit'iini mimi.¹⁶³
- 164.** Wala mimi sikutakini ujira juu yake; ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹⁶⁴
- 165.** Je! Katika viumbe vyote mnawaingilia wanaume?¹⁶⁵
- 166.** Na mnaacha alicho kuumbieni Mola wenu Mlezi katika wake zenu? Ama kweli nyinyi ni watu mnao ruka mipaka!¹⁶⁶
- 167.** Wakasema: Ewe Lut'i! Usipo acha, hapana shaka utakuwa miongoni mwa wanao tolewa mji!¹⁶⁷
- 168.** Akasema: Hakika mimi ni katika wanao kichukia hichi kitendo chenu.¹⁶⁸

sisi kwa Unabii na Utume? Na ukiwa wewe ni mkweli katika madai yako basi lete muujiza wa kuonyesha uthibitisho wa Utume wako.

155 Saleh akawaambia - alipo pewa na Mwenyezi Mungu ngamia jike kuwa ni muujiza wake: Huyu hapa ngamia jike wa Mwenyezi Mungu, amekutoleeni kuwa ni Ishara. Yeye ana sehemu yake ya maji katika siku moja; siku hiyo msinywe nyinyi. Na nyinyi mna sehemu yenu siku nyengine. Kunyweni siku hiyo.

156 Wala msimletee madhara yoyote huyu ngamia, msije mkahiliki kwa adhabu kubwa.

157 Wakamchinja ngamia, kinyume na walivyo wafikiana na Saleh. Kwa hivyo wakastahiki kuwashukia adhabu, wakawa ni wenye kujuta kwa kitendo chao hicho.

158 Basi ikawateketeza adhabu aliyo waahidi Saleh, wala majuto hayakuwakinga na adhabu ya ukosefu wao. Hakika katika kusimulia kisa chao pana dalili ya kuonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu kuwateketeza makafiri na kuwaokoa Waumini. Na si wengi katika watu wako wenye kuamini.

159 Na hakika bila ya shaka aliye kuumba ndiye Yeye Muweza wa kuwateketeza wapinzani, na Mfadhili wa kuwaokoa wachamngu.

160 Alipo waita Lut'i watu wake wamuabudu Mwenyezi Mungu pekee, na waache ushirikina, waliwakanusha Mitume wote.

161 Ewe Mtume! Watajje watu wako pale Lut'i alipo waambia watu wake, naye ni ndugu yao na shemeji yao:

162 Hakika mimi nimetumwa kwenu na Mwenyezi Mungu nikuleteeni Dini ya Haki. Nami ni muaminifu wa kuifikisha Dini hii.

163 Basi tahadarini na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na ifuateni amri yangu kwa ninayo kuitieni.

164 Wala mimi sitaki kwenu ujira kwa uwongofu na uwongozi ninao kuitieni. Sina ujira ila kwa Mwenye kumiliki viumbe vyote na Mlezi wao.

165 Lut'i alisema: Nyinyi mnastarehea kuwaingilia wanaume mkaacha wanawake? Kwa hayo anakusudia kuyakanya yale waliyo yazoea ya vitendo vichafu. (*Tazama Maelezo 26:165*)

166 Na mnaacha aliyo kuumbieni Mwenyezi Mungu ya kustarehe na wake zenu walio halali yenu? Ama hakika nyinyi ni watu mlio pindukia mipaka ya udhalimu katika kufanya maasi.

167 Walikasirika kwa kule kuwakataza na kuwakemea kwa sababu ya jambo ovu na wakasema: Kama hukuacha kutukebehi tutakutoa mji kwa izaru kubwa.

168 Lut'i akasema: Hakika mimi nakichukia mno hichi kitendo chenu, wala sitoacha kabisa kukipinga na kukikebehi.

- 169.** Mola wangu Mlezi! Niokoe mimi na ahali zangu na haya wayatendayo.¹⁶⁹
170. Basi tukamwoko ya yeye na ahali zake wote,¹⁷⁰
171. Isipo kuwa kikongwe katika walio kaa nyuma.¹⁷¹
172. Kisha tukawaangamiza wale wengine.¹⁷²
173. Na tukawanyeshea mvua, basi ni ovu mno mvua ya waliyo onywa.¹⁷³
174. Hakika katika hayo ipo Ishara. Na hawakuwa wengi wao wenye kuamini.¹⁷⁴
175. Na hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.¹⁷⁵
176. Watu wa Machakani waliwakanusha Mitume.¹⁷⁶
177. Shuaibu alipo waambia: Je! Hamfanyi mkamchamngu?¹⁷⁷
178. Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.¹⁷⁸
179. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, na nit'iini mimi.¹⁷⁹
180. Wala sikutakini ujira juu yake. Ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹⁸⁰
181. Timizeni kipimo sawa sawa, wala msiwe katika wanao punja.¹⁸¹
182. Na pimeni kwa haki iliyo nyooka,¹⁸²
183. Wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye jeuri kwa ufisadi.¹⁸³
184. Na mcheni aliye kuumbeni nyinyi na vizazi vilivyo tangulia.¹⁸⁴

169 Na akamwomba Mola wake Mlezi amwokoe yeye na ahali zake na wayatendayo wale wajinga, baada ya kwisha kata tamaa kuwa hawamsikilizi.

170 Mwenyezi Mungu akamuitikia ombi lake, akamwoko ya yeye na wale walio fuata wito wake, kwa kuwatoa wote majumbani mwao wakati wa kuteremka adhabu kuwashukia wenye kukanusha.

171 Ila mkewe kizee aliye baki, na hakutoka nao. Yeye akaangamia kwa kufuru zake na ukhaini wake, kwa kuwanga mkono wakosefu.

172 Kisha Mwenyezi Mungu akawahiliki makafiri watendao uovu kwa hilaki kali na mbaya.

173 Na Mwenyezi Mungu aliwateremshia wale watu wapotovu mawe kutoka mbinguni, yakawateketeza. Na ilikuwa mvua ya kutisha kwa wingi wake na namna yake. Basi mvua ovu ya walio kwisha onywa ni mvua hiyo, kwani iliteremka kwa uangamizi mkubwa mno!

174 Hakika adhabu ile iliyo wateremkia watu wale hapana shaka ni hoja yenye kuonyesha utimilivu wa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Wala si wengi katika watu wako wenye kusadiki hayo.

175 Na hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka ndiye Yeye Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye kusifika kwa rehema iliyo kamilika. Huwapa adhabu watendao dhambi, na huwalipa wema Waumini.

176 Hichi kisa cha Shuaibu pamoja na Watu wa Al Aykat, Machakani, nao ni msitu wenye miti mizuri, karibu na Madian. Kikundi cha watu waliteremkia hapo na wakakaa. Mwenyezi Mungu akawapelekea Shuaibu kama alivyo wapelekea watu wa Madian. Wakamkadhibisha katika wito wake. Na kwa hivi wakawa wamekanusha risala za Mitume wote.

177 Ewe Muhammad! Watajie watu wako pale Shuaibu alipo waambia watu wa Machakani: Je! Hamumkhofu Mwenyezi Mungu mkamuamini? Wakaingia kumkadhibisha.

178 Hakika mimi nimetumwa na Mola Mlezi wa walimwengu wote nikuongoeni na nikuongozeni. Nami ni muaminifu wa kuufikisha ujumbe wake kwenu.

179 Basi tahadharini na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na nit'iini kwa kufuata amri za Mwenyezi Mungu, na kuziokoa nafsi zenu na madhambi.

180 Na mimi kwa hivi kukuongozeni na kukufunzeni sikutakini ujira wowote. Mimi sina malipo kaamili kwa sababu ya kazi yangu ila kutokana na Mola Mlezi wa walimwengu wote.

181 Shuaibu akawaamrisha kutimiza vipimo kwa ukamilifu wanapo pima, kwani ilikuwa ada yao kupunguza kwa pishi na mizani, kupunguza haki za watu kwa kuwapunja na kuwapimia kasoro.

182 Na wapimieni watu kwa mizani ya sawa sawa, ili wachukue haki yao kwa uadilifu ulio nyooka.

183 Wala msiwapunguzie watu haki zao, wala msipite katika nchi mkifisidi kwa kuuwa, na uharamia, na kufanya madhambi, na kufuata pumbao.

184 Na tahadharini na adhabu ya Mwenyezi Mungu aliye kuumbeni, na akaumba kaumu zenye nguvu na

- 185.** Wakasema: Hakika wewe ni katika walio rogwa.¹⁸⁵
- 186.** Na wewe si chochote ila ni mtu tu kama sisi, na kwa yakini tunakuona wewe ni katika waongo.¹⁸⁶
- 187.** Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.¹⁸⁷
- 188.** Akasema: Mola wangu Mlezi anajua zaidi mnayo yatenda.¹⁸⁸
- 189.** Basi walimkanusha, na ikawashika adhabu ya siku ya kivuli. Hakika hiyo ilikuwa adhabu ya siku kubwa.¹⁸⁹
- 190.** Hakika katika hayo ipo Ishara, lakini hawakuwa wengi wao wenye kuamini.¹⁹⁰
- 191.** Na hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka ndiye Yeye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.¹⁹¹
- 192.** Na bila ya shaka hii ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹⁹²
- 193.** Ameuteremsha Roho muaminifu,¹⁹³
- 194.** Juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji,¹⁹⁴
- 195.** Kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi.¹⁹⁵
- 196.** Na hakika bila ya shaka haya yamo katika Vitabu vya kale.¹⁹⁶
- 197.** Je! Haikuwa kwao ni Ishara kwamba wanayajua haya wanazuoni wa Wana wa Israili?¹⁹⁷
- 198.** Na lau kuwa tungeli iteremsha juu ya mmoja wa wasio kuwa Waarabu,¹⁹⁸

takaburi zilizo tangulia.

185 Wakasema: Wewe si chochote ila ni mtu aliye sibiwa na uchawi mkali na ikapotea akili yake.

186 Na wewe si chochote ila ni mmoja wetu sawa na sisi kwa utu. Basi vipi ujipe ubora kuliko sisi kwa Utume? Nasi tunaamini kuwa wewe ni mwongo wa kuboea.

187 Basi hebu tuangushie vipande vya adhabu kutoka mbinguni ikiwa ni katika wasemao kweli kwa huu ujumbe wako! Na chini ya shauri hii kwa hakika pana kila namna ya ubishi.

188 Shuaibu akasema: Mola wangu Mlezi ni Mjuzi, upeo wa kujua, wa maasi yote myatendayo, na adhabu mnayo stahiki. Yeye atakuteremshieni hayo kwa wakati wake alio ukadiria. Na huu ndio hadi ya mwisho wa kumwachilia Mwenyezi Mungu kila kitu, na kuwatisha hao makafiri.

189 Lakini wao waliendelea kumkadhibisha. Mwenyezi Mungu akawapatiliza kwa adhabu ya joto kuu mno. Wakawa wanatapa tapa hawana pa kukimbilia. Walipo pata kiwingu cha kuwapa kivuli kuinga mwako wa jua walijikusanya chini yake. Mwenyezi Mungu akawateremshia moto, ukawateketeza wote katika siku ya kitisho kikubwa mno.

190 Hakika adhabu iliyo wateremkia watu wa Machakani kuwa ni malipo ya uasi wao, ni dalili ya ukamilifu wa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Na hawakuwa wengi wa watu wako wenye kusadiki.

191 Na hakika Mola wako Mlezi hapana shaka ndiye Yeye aliye tengeka kwa Nguvu na Ushindi, Mwenye kuwaneemesha Waumini kwa rehema nyingi.

192 Na hakika hii Qur'ani iliyo tajwa ndani yake visa vya kweli imeteremshwa kutoka kwa Mwenye kuumba walimwengu wote, Mwenye kumiliki mambo yao, na Mlezi wao. Basi khabari zake ni za kweli. Na hukumu yake inatimizwa mpaka Siku ya Kiyama.

193 Ameiteremsha Roho muaminifu, naye ni Jibril a.s.,

194 Juu ya moyo wako ulio tulia kuihifadhi na kuifahamu, na idhibitike katika moyo wako iwe madhubuti isisahaulike, ili upate kuwaonya wakhalifu kwa adhabu ziliomo ndani yake.

195 Jibril amekuteremshia kwa lugha ya Kiarabu, yenye maana wazi, yenye hoja zilizo dhaahiri kwa wanayo hitajia ya kutengeneza mambo yao ya dunia na Dini.

196 Na hakika kuitaja Qur'ani na kueleza kuwa inatoka kwa Mwenyezi Mungu kumteremshia Muhammad s.a.w. yametajwa katika Vitabu vya Manabii walio tangulia.

197 Je! Hawa wenye inda wanaikataa Qur'ani na hali wao wanayo hoja inayo onyesha ukweli wa Muhammad s.a.w., nayo ni ilimu ya wanazuoni wa Wana wa Israili juu ya Qur'ani kama ilivyo katika vitabu vyao?

198 Na lau tungeli mteremshia mtu asiye kuwa Mwaarabu, anaye weza kusema Kiarabu lakini si kwa

199. Na akawasomea, wasingeli kuwa wenye kuamini.¹⁹⁹
200. Namna hivi tunaingiza katika nyoyo za wakosefu.²⁰⁰
201. Hawataimini mpaka waione adhabu chungu.²⁰¹
202. Basi itawafikia kwa ghafla, na hali hawana khabari.²⁰²
203. Na watasema: Je, tutapewa muhula?²⁰³
204. Basi, je, wanaihimiza adhabu yetu?²⁰⁴
205. Waonaje kama tukiwastarehesha kwa miaka,²⁰⁵
206. Kisha yakawafikia waliyo kuwa wakiahidiwa,²⁰⁶
207. Yatawafaa nini yale waliyo stareheshewa?²⁰⁷
208. Wala hatukuangamiza mji wo wote ila ulikuwa na waonyaji-²⁰⁸
209. Kuwa ni ukumbusho. Wala Sisi hatukuwa wenye kudhulumu.²⁰⁹
210. Wala Mashet'ani hawakuteremka nayo,²¹⁰
211. Wala haitakiwi kwao, na wala hawawezi.²¹¹
212. Hakika hao wametengwa na kusikia.²¹²
213. Basi usimwombe mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu ukawa miongoni mwa watacao adhibiwa.²¹³
214. Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe.²¹⁴
215. Na watwae kwa upole wanao kufuata miongoni mwa Waumini.²¹⁵

ufasihi, wasingeli waza kumtuhumu kuwa kaizua.

199 Na angeli wasomea baraabara kinyume na ada bado wangeli mkanusha, na wakapatia kisababu kwa ukafiri wao.

200 Sisi tumekutia huko kukanusha katika nyoyo za wakosefu; na tumekuthibitisha kama tulivyo kuthibitisha katika nyoyo za wenye sifa kama zao.

201 Basi hapana njia ya wao kuacha tabia yao ya ukafiri mpaka wateseke kwa hiyo adhabu kali walio ahidiwa.

202 Itawateremkia adhabu kwa ghafla bila ya kuitaraji, wala wao hawajui kama inakuja.

203 Watasema itapo teremka hiyo adhabu: Je, tutapewa muhula? Haya ni kwa majuto kwa kupitiwa na Imani na kutaka waakhirishiwe adhabu. Lakini hawajibiwi.

204 Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Watu wa Makka wameghurika na kuchelewesha kwangu kuwaadhibu, basi ndio wanaihimiza? Anakusudia *Subhanahu* Aliye takasika kuzisafihii akili zao kwa sababu ya kuhimiza kwao adhabu juu ya kuwaonya na kuwatisha.

205 Je, umefikiri ukajua, kama Sisi tuliwastarehesha kwa uhai kwa muda wa miaka mingi pamoja na maisha mema?

206 Kisha ikawateremkia adhabu iliyo ahidiwa.

207 Kustarehe kwao kwa umri mrefu na maisha mema hakutowakinga hata chembe na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Kwani adhabu ya Mwenyezi Mungu itakuja tu, kama si leo kesho. Wala hapana kheri katika neema ambayo khatima yake ni adhabu.

208 Na mwendo wetu kwa kaumu zote ni kuwa hatuuteketezi umma ila baada ya kuwatumia Mitume wa kuwaonya kwa kufuata hoja.

209 Wakumbuke na wazingatie. Wala si shani yetu kudhulumu hata tuuadhibu umma kabla ya kuwaletea Mtume.

210 Qur'ani inakataa waliyo yasema makafiri wa Makka ya kwamba Muhammad anafuata majini, nao ndio wanampa Qur'ani. Qur'ani inasema: Mashetani hawakuteremsha hii Qur'an.

211 Wala haiwafalii wao kuteremsha, na hawawezi kufanya hivyo.

212 Kwani hao hakika wanazuiwa wasiisikie Qur'ani pale inapo funuliwa kwa Muhammad s.a.w.

213 Basi wewe muelekee Mwenyezi Mungu ukiendelea na usafi wako wa ibada, wala usishughulike na fisadi za madai ya washirikina na mwendo wao muovu. Na hivi kutakiwa Mtume s.a.w. awe na ikhlasi ya namna hii ni wito kwa jamii ya watu waliomo katika umma wake.

214 Watie khofu ya adhabu ya shirki na maasi walio karibu nawe katika jamaa zako.

215 Na kuwa mpole kwa wanao itikia wito wako wa Imani.

216. Na ikiwa watakuasi basi sema: Mimi najitenga mbali na hayo mnayo yatenda.²¹⁶
217. Na umtegemee Mtukufu Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.²¹⁷
218. Ambaye anakuona unapo simama,²¹⁸
219. Na mageuko yako kati ya wanao sujudu.²¹⁹
220. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua.²²⁰
221. Je! Nikwambieni nani wanawashukia Mashet'ani?²²¹
222. Wanamshukia kila mzushi mkubwa mwingi wa dhambi.²²²
223. Wanawapelekea yale wanayo yasikia; na wengi wao ni waongo.²²³
224. Na watungaji mashairi ni wapotofu ndio wanawafuata.²²⁴
225. Je! Huwaoni kwamba wao wanatangatanga katika kila bonde?²²⁵
226. Na kwamba wao husema wasiyo yatenda?²²⁶
227. Isipo kuwa wale walio amini, na wakatenda mema, na wakamkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi, na wakajitetea wanapo dhulumiwa. Na wanao dhulumu watakuja juu mgeuko gani watakao geuka.²²⁷

216 Pindi wakikuasi na wasikufuate basi jitenge nao, na jitenge na vitendo vyao vya ushirikina na maasi yote.

217 Na tegemeza mambo yako kwa Mwenye nguvu, Mwenye uweza wa kuwatenda nguvu adui zako kwa utukufu wake, na kukunusuru wewe na kumunusuru kila mwenye kufanya a'mali yake kwa usafi wa niya.

218 Ambaye anakuona pale unapo simama kwa ibada za usiku na vitendo vyote vya kheri.

219 Na anaona mwendo wako kati ya wanao sali, kwa kusimama, na kukaa, na kurukuu na kusujudu, pale unapo waongoza katika Sala.

220 Hakika Yeye *Subhanahu* ndiye Mwenye kusikia dua zako na dhikri zako, ndiye Mjuzi wa kujua niya yako na vitendo vyako. Ni kama kwamba *Subhanahu* anamwambia: Usichukue taklifi kubwa bila ya kiasi katika mashaka ya ibada, kwani uyatendayo yote nayaona na nayasikia Mimi.

221 Washirikina walisema: Mashetani ndio wanamsomea Qur'ani Muhammad. Qur'ani ikawajibu: Nikupeni khabari watu gani Mashetani ndio wanawateremkia, na wakawashawishi.

222 Wanamteremkia kila mwenye kubeba dhambi za namna mbaya kabisa za uwongo, na madhambi ya kuchusha kabisa. Nao ni hao makohani mafisadi ambao tabia zao na tabia za Mashetani ni jinsi moja na zimewafikiana.

223 Hao hutega masikio yao kwa Mashetani, na kwao wapakata mambo ya dhana dhana tu. Na wengi wao ni waongo, na huzidisha tena juu ya kauli walizo zipata kwa Mashetani.

224 Makafiri wanasema: Hii Qur'ani ni mashairi, na Muhammad ni mtungaji mashairi. Mwenyezi Mungu ameyavunja haya kwa kuthibitisha kuwa hakika Qur'ani imejaa hikima na hukumu. Mpango wake unapingana na mpango wa mashairi ambao unategemea juu ya kweli na uwongo. Na amebainisha kwamba hali ya Muhammad s.a.w. inapingana na hali ya watungaji mashairi. Yeye anasema kwa hikima, wao wanasema kwa udanganyifu. Na hii ndiyo hali ya wengi katika watungaji mashairi.

225 Kwani huwaoni vile wanavyo tangatanga katika mabonde ya maneno wala hawaongoki kwenye Haki?

226 Na kwamba wao husema kwa ndimi zao wasio yaambatisha na vitendo vyao?

227 Lakini walio hidika kwa hidaya ya Mwenyezi Mungu, na wakatenda mema mpaka zikatua katika nafsi zao sifa bora, na wakamkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi mpaka ikathibiti khofu katika nyoyo zao, hawa basi huyafanya mashairi kama dawa ilio sibu kwa ugonjwa wake. Na hupambana kwa ajili ya kuiwania Dini yao na kusimamisha Haki, inapo kuwa Haki inafanyiwa jeuri. Na walio dhulumu nafsi zao kwa shirki na kumkejeli Mtume kwa mashairi, watatafuta wapi pa kuikimbia shari na hilaki wanayo ienda.

Sura 27 - An-Naml

Utangulizi

SURA AN-NAML ni ya Makka. Aya zake ni 93.

Imeanza kwa harufi za kutamkwa, kukumbusha cheo cha Qur'ani ambayo imetoka katika jinsi ya maneno ya Kiarabu. Na juu ya hivyo imewashinda hao Waarabu kuleta mfano wake. Na tena pia ni kama kumzindua aliye ghaflika aisikilize. Baada yake kimekuja kisa cha Musa a.s. Na imetajwa baadhi ya miujiza yake, na kisa cha Daudi a.s. na kurithiwa kwake na mwanawe, Mfalme Sulaiman, na kukusanyika majini, na watu, na ndege kwa ajili yake. Na imetajwa kufahamu kwake Sulaiman maneno ya wanyama, na shukrani yake kwa neema hii. Kisha kutoweka ndege Hud-hud, na akaja na kisa cha Balqis, na kuabudu kwake bibi huyu na watu wake kuliabudu jua. Tena Sulaiman akampelekea barua, naye akamjibu kwa kumpelekea zawadi baada ya kushauriana na watu wake, na ikaelezwa kuletwa kiti chake cha enzi kwa njia ya mwenye ilimu ya Kitabu, na kuingia kwake huyo bibi katika qasri (jumba la kifalme) la Sulaiman, nalo likamshitua, na akatangaza ut'iifu wake na Imani yake kumuamini Sulaiman.

Na Sura hii imetaja hadithi ya Saleh a.s. na kaumu yake, na hadithi ya Lut'i a.s. na kaumu yake, na kuvuka kwake, na kuangamia kwa mafisadi. Na Sura tukufu hii imezindua ziangaliwe dalili za aliye umba mbingu na ardhi zenye kuthibitisha uwezo wake na upweke wake.

Na ikaashiria cheo cha Qur'ani tukufu katika kazi ya Daa'wa (Wito), na vipi washirikina wanavyo ipuza juu ya kuwa muujiza wake umekamilika. Na imetaja yatakayo kuwa atapo toka mnyama akisema na watu kuwa walikuwa hawana yakini ya Ishara zetu. Kisha Sura ikaelekea ulimwengu, na vipi watavyo fazaika waliomo wakati wa mpulizo wa kufufuliwa na kukusanywa. Na ikanabihisha hali ya ardhi, na kwamba milima yake inakwenda kama yaendavyo mawingu, na ikasimulia yanayo mfuatia Mtume katika kazi yake ya Daa'wa, na kwamba ni waajibu Mwenyezi Mungu Aliye takasika asifiwe.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. T'aa Siin. (T'.S.), Hizi ni Aya za Qur'ani na Kitabu kinacho bainisha;¹
2. Uwongofu na bishara kwa Waumini,²
3. Ambao wanashika Sala, na wanatoa Zaka, na Akhera wana yakini nayo.³
4. Kwa hakika wale wasio iamini Akhera tumewapambia vitendo vyao, kwa hivyo

1 T'aa Siin, (T' na S) harufi mbili za kutamkwa, ni harufi za alifbete, ndizo zimeanzia Sura hii, ili kunabihisha siri ya muujiza wa Qur'ani pamoja na kuashiria kuwa imeundwa kwa jinsi ya harufi hizi hizi mnazo zitumia katika kusema, na pia kuzindua akili zisikilize hii Qur'ani inapo somwa. Hizi Aya zilizo teremka kwa kusomwa, na ni Kitabu chenye kubainisha mambo yaliyo kuja ndani yake.

2 Na hii Qur'ani ni Uwongofu wa kuwaahidi Waumini waifuate njia ya kheri, na kufuzu duniani na Akhera, na inawabashiria kuwa watapata malipo mazuri.

3 Waumini hao ndio wanao ishika Sala kwa unyenyekevu na kutimiliza nguzo, na wanatoa Zaka kwa nyakati zake, nao wana yakini ya maisha ya baadaye Akhera, na yatayo kuwa huko ya adhabu na thawabu.

wanatangatanga ovyo.⁴

5. Hao ndio watapata adhabu mbaya kabisa, na hao katika Akhera ndio watapata khasara zaidi.⁵

6. Na hakika wewe unafundishwa Qur'ani inayo tokana kwake Mwenye hikima Mwenye kujua.⁶

7. (Kumbuka) Musa alipo waambia ahali zake: Hakika nimeona moto, nitakwenda nikuleteeni khabari, au nitakuleteeni kijinga kinacho waka ili mpate kuota moto.⁷

8. Basi alipo fika ilinadiwa: Amebarikiwa aliomo katika moto huu na walioko pembezoni mwake. Na ametakasika Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁸

9. Ewe Musa! Hakika Mimi ndiye Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.⁹

10. Na itupe fimbo yako! Alipo iona ikitikisika kama nyoka, aligeuka nyuma wala hakungoja. Ewe Musa! Usikhofu! Hakika hawakhofu mbele yangu Mitume.¹⁰

11. Lakini aliye dhulumu, kisha akabadilisha wema baada ya ubaya, basi Mimi ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.¹¹

12. Na ingiza mkono wako katika mfuko wako, utatoka mweupe bila ya maradhi. Ni katika Ishara tisa za kumpelekea Firauni na kaumu yake. Hakika hao walikuwa watu waovu.¹²

13. Basi zilipo wafikia Ishara zetu hizo zenye kuonyesha, wakasema: Huu ni uchawi dhaahiri.¹³

14. Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!¹⁴

4 Hakika wale ambao hawaiamini Akhera, Sisi tumewapambia vitendo vyao kwa kuwaambia matamanio ndani yake. Kwa hivyo wao wanababaika humo katika upotovu wao.

5 Hao ndio watapata adhabu mbaya kabisa, na Akhera ndio watakuwa khasarani kushinda wote.

6 Ewe Nabii! Wewe unapokea Qur'ani hii unayo teremshiwa kutokana na Yeye ambaye hapana anaye mkaribia kwa hikima yake, naye anajua kila kitu.

7 Kumbuka pale Musa alipo mwambia mkewe na walio pamoja naye na yeye ndio anarejea Misri: Mimi nimeona moto. Nitakwenda kuleteeni khabari ya njia, au nitapata kijinga cha moto, kitacho kufaeni kwa kuota moto kwa hii baridi.

8 Alipo fika huko paliitwa: Wamebarikiwa waliomo katika moto huu na walioko pembezoni mwake, yaani karibu yake. Nao ni Malaika na Musa. Na Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote ametakasika na kila kisicho kuwa laiki naye.

9 Ewe Musa! Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu, Mwenye kustahiki kuabudiwa pekee, Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye kuweka kila kitu pahala pake.

10 Na katika njia ya kufikisha wito wako, tupa fimbo yako na utaiona inatikisika kama kijoka jepesi kinakwenda mbio. Yeye akarudi nyuma, wala hakurejea baada ya kurudi nyuma. Mwenyezi Mungu Mtukufu akamtua kwa kauli yake: Usiogope. Mbele yangu hawaogopi. Mitume ninapo sema nao. (*Tazama Maelezo 27:10*)

11 Lakini mwenye kutenda asicho ruhusiwa, na kisha akaleta wema baada ya kuteleza kwake, basi Mimi ni Mwingi wa kusamehe, Mkubwa wa kurehemu.

12 Na utie mkono wako katika mfuko wa nguo zako, utatoka mweupe wala si kwa balanga. Hayo ni katika Ishara tisa za kumpelekea Firauni na kaumu yake. Hakika hao walikuwa watu walio tokana na amri ya Mwenyezi Mungu, ni makafiri. (*Tazama Maelezo 27:12*)

13 Ilipo kuja miujiza hii kwa uwazi na dhaahiri wakasema: Huu ni uchawi wazi!

14 Wakaikadhibisha miujiza wakikataa kuwa inaonyesha dalili ya Utume. Na hakika yakini ilikwisha waingia katika nyoyo zao, lakini hawakusalimu amri kwa kuwa walikwisha tangaza kufuata upotovu na kushika uasi. Basi ewe Nabii! Hebu angalia vipi yalikuwa matokeo ya walio shikilia ufasidi, wakaikanya

15. Na hakika tuliwapa Daudi na Sulaiman ilimu, na wakasema: *Alhamdu Lillahi*, Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu aliye tufadhilisha kuliko wengi katika waja wake Waumini.¹⁵
16. Na Sulaiman alimrithi Daudi, na akasema: Enyi watu! Tumefunzwa usemi wa ndege, na tumepewa kila kitu. Hakika hii ni fadhila iliyo dhaahiri.¹⁶
17. Na alikusanyiwa Sulaiman majeshi yake ya majini, na watu, na ndege; nayo yakapangwa kwa nidhamu.¹⁷
18. Mpaka walipo fika kwenye bonde la wadudu chungu, alisema mdudu chungu mmoja: Enyi wadudu chungu! Ingieni majumbani mwenu, asikupondeneni Sulaiman na majeshi yake bila ya wao kutambua.¹⁸
19. Basi (Sulaiman) akatabasamu akacheka kwa neno hili, na akasema: Ee Mola wangu Mlezi! Nizindue niishukuru neema yako uliyo nineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kutenda mema uyapendayo, na uniingize kwa rehema yako katika waja wako wema.¹⁹
20. Na akawakagua ndege, na akasema: Imekuwaje, mbona simwoni Hud-hud, au amekuwa miongoni mwa walio ghibu?²⁰
21. Kwa yakini nitamuadhibu kwa adhabu kali, au nitamchinja, au aniletee hoja ya kutosha.²¹
22. Basi (Hud-hud) akakaa si mbali na akasema: Nimegundua usilo gundua wewe, na ninakujia hivi kutoka nchi ya Sabai, na nakuletea khabari za yakini.²²
23. Hakika mimi nimemkuta mwanamke anawatawala, naye amepewa kila kitu, na anacho kiti cha enzi kikubwa.²³

miujiza nayo iko wazi.

15 Hizo ndizo jeuri za Firauni kwa sababu ya ufalme wake. Hebu sasa angalia utawala muadilifu, utawala wa hukumu, utawala wa unabii wa Daudi na mwanawe, Sulaiman, Mwenyezi Mungu awape amani. Sisi tuliwapa ilimu nyingi za sharia na mazoezi ya kuhukumu. Wakasimamisha uadilifu, na wakamhimidi Mwenyezi Mungu aliye wapa fadhila kushinda wengi katika waja wake wenye kusadiki, na kuifuata Haki.

16 Ufalme na hukumu ukatoka kwa Daudi ukenda kwa mwanawe, Sulaiman; naye akasema: Enyi watu! Sisi tumefunzwa lugha ya ndege, na tumepewa mengi tunayo yahitajia katika utawala wetu. Hakika neema hizi ni fadhila iliyo wazi aliyo tukhusisha sisi Mwenyezi Mungu, (*Tazama Maelezo 27:16*)

17 Na Sulaiman alikusanya majeshi yake ya majini, watu, na ndege, kwenye uwanja mmoja. Na wao wakawa jeshi moja lenye nidhamu kwa vile kudhibitiwa wa mwanzo mpaka mwisho.

18 Hata walipo fika kwenye bonde la wadudu chungu, mdudu chungu mmoja akasema: Enyi wadudu chungu! Ingieni vishimoni mwenu, asije Sulaiman na askari wake wakakuweni na wao wala hawahisi kuwa nyinyi mpo. (*Tazama Maelezo 27:18*)

19 Sulaiman akatabasamu akicheka kwa ile kauli ya mdudu chungu yenye kushughulikia maslaha yao, na akahisi neema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu iliyo juu yake. Akasema: Ewe Uliye niumba! Nijaalie niwe na shukrani kwako kwa neema ulizo nineemesha mimi na wazazi wangu, na niwezeshe nitende vitendo vyema unavyo viridhia, na unitie kwenye rehema yako iliyo timia.

20 Akalikagua jeshi lake la ndege asimwone Hud-hud. Akastaajabu, akasema: Mbona simwoni Hud-hud! Yupo hapa na mimi simwoni, au ameghibu hayupo miongoni mwetu?

21 Wallahi! Nitampatisha adhabu kali ya kumshikisha adabu, au nitamchinja ikiwa kosa lake ni kubwa! Ila aniletee hoja madhubuti ya kumtoa makosani kwa kuto kuwepo mbele yangu.

22 Na Hud-hud alikuwa kakaa si pahala mbali kwa muda usio kuwa mrefu. Kisha akamjia Sulaiman, akamwambia: Nimejua jambo ulilo kuwa wewe hujalijua, na nimekujia kutoka nchi ya Sabai na khabari muhimu sana, nayo ni ya kweli kwa yakini. (*Tazama Maelezo 27:22*)

23 Hakika mimi nimewaona watu wa Sabai wanatawaliwa na mwanamke, na amepewa kila kheri za kidunia, naye ana kiti cha enzi kikubwa kinacho onyesha dalili ya utukufu wa ufalme na nguvu za madaraka yake.

24. Nimemkuta yeye na watu wake wanalisujudia jua badala ya Mwenyezi Mungu; na Shet'ani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia Njia. Kwa hivyo hawakuongoka,²⁴
25. Na hawamsujudii Mwenyezi Mungu ambaye huyatoa yaliyo fichikana katika mbingu na ardhi, na anayajua mnayo yaficha na mnayo yatangaza.²⁵
26. Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi tukufu.²⁶
27. Akasema (Sulaiman): Tutatazama umesema kweli au wewe ni miongoni mwa waongo.²⁷
28. Nenda na barua yangu hii na uwafikishie, kisha waache na utazame watarejesha nini.²⁸
29. (Malkia) akasema: Enyi wahishimiwa! Hakika nimeletewa barua tukufu.²⁹
30. Imetoka kwa Sulaiman nayo ni: Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.³⁰
31. Msinifanyie jeuri, na fikenii kwangu nanyi mmekwisha kuwa wenye kusalimu amri.³¹
32. Akasema: Enyi wahishimiwa! Nipeni shauri katika jambo langu hili, kwani mimi sikati shauri yoyote mpaka mhudhurie.³²
33. Wakasema: Sisi ni wenye nguvu na wakali kwa vita; na amri iko kwako, basi tazama ni nini unaamrisha.³³
34. Akasema: Hakika wafalme wanapo uingia mji wanauharibu, na wanawafanya wale watukufu wake kuwa wanyonge. Na hivyo ndivyo watendavyo.³⁴
35. Lakini mimi nitawapelekea zawadi, nami nitangoja watakayo rudi nayo wajumbe.³⁵
36. Basi alipo fika (mjumbe) kwa Sulaiman, alisema (Sulaiman): Hivyo ndio nyinyi mnanisaidia kwa mali? Aliyo nipa Mwenyezi Mungu ni bora zaidi kuliko aliy kupeni

24 Nimemwona yeye na watu wake wanaabudu jua, wala hawamuabudu Mwenyezi Mungu. Na Shetani amewazainishia vitendo vyao na wenyewe wakaviona ni vizuri na hali ni viovu. Kwa hivyo amewapoteza Njia ya Haki, basi hawakuongoka.

25 Hawamsujudii Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye ndiye anayafichua yaliyo fichika katika mbingu na ardhi, na anajua mnayo fanya kwa siri na kwa dhaahiri.

26 Mwenyezi Mungu, ambaye hapana wa kuabudiwa kwa Haki isipo kuwa Yeye, ndiye Mwenye madaraka makuu yasio na ukomo juu ya kila kiumbe.

27 Sulaiman akasema kumwambia Hud-hud: Tutaichungua khabari yako hii tujue kwamba umesema kweli au wewe ni miongoni mwa waongo.

28 Nenda na barua yangu hii umfikishie yeye na kaumu yake. Kisha jitenge nao ujifiche pahali karibu, uangalie wanarejesheana maneno gani.

29 Barua ikamfikia yule Malkia, naye basi akawakusanya wahishimiwa wa kaumu yake, na halmashauri wake. Naye akasema: Enyi wahishimiwa! Mimi hakika imenifikilia barua yenye shani kuu.

30 Kisha akawasomea hiyo barua, nayo imeanzia kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye utukufu na neema zote, ambaye daima anawamimnia waja wake rehema zake.

31 Msifanye kiburi juu yangu, na nijieni nanyi mmet'ii na wanyenyekevu.

32 Akaiambia baraza ya washauri wake: Nibainishieni lifaalo katika haya mambo muhimu nilio wekewa mbele yangu. Kwani mimi sikati shauri juu ya jambo lolote mpaka muwe nyinyi mmehudhuria.

33 Wakamwambia nao wametua: Sisi ni watu wenye nguvu za mwili, na tuna moyo na mashujaa. Hatuogopi vita. Basi angalia wewe jambo unalo taka kutuamrisha nasi ni wenye kut'ii.

34 Akasema kwa taratibu na kupendelea salama: Hakika watawala wakiingia katika miji mikubwa pamoja na majeshi yao huifisidi, wakaondoa matengenezo yake, wakateketeza makulima na roho, na wakawafanya walio watukufu katika watu wa hiyo miji kuwa ndio madhalili, na huo ndio mtindo wao daima.

35 Na mimi kwa kupendelea salama na uzima nitampelekea zawadi Sulaiman na kaumu yake, na nitatazama wajumbe watarejea na nini - wataikubali zawadi au watairudisha?

nyinyi. Lakini nyinyi mnafurahia hii zawadi yenu.³⁶

37. Rejea kwao! Kwa yakini sisi tutawajia kwa majeshi wasio yaweza kuyakabili. Na hakika tutawatoa humo na hali wao wamekuwa madhalili na wanyonge.³⁷

38. Akasema: Enyi wahishimiwa! Ni nani kati yenu atakaye niletea kiti chake cha enzi kabla hawajanijia nao wamekwisha salimu amri.³⁸

39. Akasema: Afriti, katika majini: Mimi nitakuletea kabla hujainuka pahala pako hapo. Na mimi kwa hakika nina nguvu na muaminifu.³⁹

40. Akasema mwenye ilimu ya Kitabu: Mimi nitakuletea kabla ya kupepesa jicho lako. Basi alipo kiona kimewekwa mbele yake, akasema: Haya ni katika fadhila zake Mola wangu Mlezi, ili anijaribu nitashukuru au nitakufuru. Na mwenye kushukuru, kwa hakika, anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake; na anaye kufuru, kwa hakika Mola wangu Mlezi ni Mkwasi na Karimu.⁴⁰

41. Akasema: Mgeuzieni kiti chake cha enzi hiki, tuone ataongoka, au atakuwa miongoni mwa wasio ongoka.⁴¹

42. Basi (Malkia) alipo fika akaambiwa: Je! Kiti chako cha enzi ni kama hiki? Akasema: Kama kwamba ndicho hichi. (Sulaiman na watu wake wakasema): Na sisi tumepewa ilimu kabla yake (Malkia), na tukawa Waislamu.⁴²

43. Na yale aliyokuwa akiyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu yalimzuilia. Hakika yeye (Malkia) alikuwa katika kaumu ya makafiri.⁴³

44. Akaambiwa: Liingie behewa la hili jumba. Alipo liona alidhani ni maji, na

36 Wajumbe walifika kwa Sayyidina Sulaiman na zawadi zao. Huku anazijua neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu zililo juu yake, Akawaambia naye ndio anamsemeza huyo Malkia na watu wake katika mkabala na wajumbe: Hivyo ndio mnanipa mimi mali? Aliyo nipa Mwenyezi Mungu ya Unabii, na ufalme, na neema, ni makubwa zaidi kuliko aliyokuwa kupeni nyinyi. Bali nyinyi kwa hizi zawadi zenu na wingi wa mali yenu mnafurahi, sio kama mimi. Kwa sababu nyinyi hamjui ila yaliyo shikamana na dunia hii tu.

37 Akasema, akimsemeza yule msemaji kwa jina lao: Ewe mjumbe! Rejea kwao. Wallahi! tutawatokea kwa majeshi wasio yaweza kupambana nayo na kuyakabili. Na tutawatoa kwenye nchi ya Sabai nao wamepoteza utukufu wao, wamefanywa watumwa.

38 Sulaiman akawaelekea binaadamu na majini aliyokuwa dhalilishiwa na Mwenyezi Mungu kumtumikia, akawashitua kwa jambo geni. Akasema: Ni nani katika nyinyi anaweza kuniletea kiti chake cha enzi kikubwa kabla hawajanijia nao wamekwisha nyenyekeka wanat'ii.

39 Mmoja pandikizi la kijini lilisema: Mimi nitakuletea, na wewe umekaa katika baraza yako hii, kabla hujaondoka. Na mimi hakika naweza hayo, na muaminifu katika maneno yangu na vitendo vyangu.

40 Akasema aliye pewa nguvu za kiroho, na ilimu ya Kitabu: Mimi nitakuletea hicho kiti cha enzi kabla jicho lako halijapepesa. Na akatimiza aliyoyasema. Sulaiman alipo kiona kiti kile kimetua mbele yake bila ya mtingisiko, alisema: Haya ni katika fadhila za Mwenyezi Mungu aliye niumba na akanipa kheri zake ili anifanyie mtihani, nitashukuru kwa neema hizi au sitoi haki yake? Na mwenye kumshukuru Mwenyezi Mungu basi huyo hakika amejiondolea nafsi yake mzigo wa waajibu. Na mwenye kuacha kushukuru kwa neema basi hakika Mola wangu Mlezi ni Mkwasi, si mwenye kuhitajia shukrani. Naye ni Karimu wa kuneemsha.

41 Sulaiman akawaambia watu wake: Kigeuzeni geuzeni hichi kiti cha enzi kwa baadhi ya mabadiliko ya nje, tupate kuona atakijua kwa kukiendea au hato kijua na kwa hivyo hato kiendea.

42 Alipo fika jicho lake lilipiga kwenye kiti chake cha enzi. Akaambiwa: Je! Kiti chako cha enzi ni mfano wa hiki? Akasema kwa vile kilivyo kamilika kufanana: Kama kwamba ndicho hichi. Na Sulaiman na walio pamoja naye wakasema: Sisi tulisha pewa ujuzi kumjua Mwenyezi Mungu na uwezo wake na ukweli wa yaliyo kuja kutoka kwake kama anavyo jua mwanamke huyu. Na sisi tangu hapo ni watu tulio mfuata Mwenyezi Mungu na tunamsafia Yeye ibada.

43 Na zile ibada za jua na mfano wake zilimzuia yule Malkia kumuabudu Mwenyezi Mungu. Kwani yeye alikuwa katika kaumu ya makafiri.

akapandisha nguo mpaka kwenye miundi yake. (Sulaiman) akasema: Hakika hilo ni behewa lilio sakafiwa kwa viyoo! Akasema (Malkia): Mola wangu Mlezi! Mimi nimejidhulumu nafsi yangu, na sasa nanyenyekea pamoja na Sulaiman kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁴⁴

45. Na kwa kina Thamud tulimtuma ndugu yao Saleh kuwaambia: Muabuduni Mwenyezi Mungu. Basi wakawa makundi mawili yanayo gombana.⁴⁵

46. Akasema: Enyi watu wangu! Kwa nini mnauhimiza uwovu kabla ya wema? Kwa nini hamuombi msamaha kwa Mwenyezi Mungu ili mrehemewe?⁴⁶

47. Wakasema: Tuna kisirani nawe na wale walio pamoja nawe. Yeye akasema: Uguzi wa ukorofi wenu uko kwa Mwenyezi Mungu; lakini nyinyi ni watu mnao jaribiwa.⁴⁷

48. Na walikuwamo mjini watu tisa wakifanya ufisadi katika nchi wala hawafanyi la maslaha.⁴⁸

49. Wakasema: Apishaneni kwa Mwenyezi Mungu tutamshambulia usiku yeye na ahali zake; kisha tutamwambia mrithi wake: Sisi hatukuona maangamizo ya watu wake, na sisi bila ya shaka tunasema kweli.⁴⁹

50. Basi wakapanga mipango yao, na Sisi tukapanga mipango yetu, na wao hawatambui.⁵⁰

51. Basi angalia ulivyo kuwa mwisho wa mipango yao, ya kwamba tuliwaangamiza wao pamoja na watu wao wote.⁵¹

52. Basi hizo nyumba zao ni tupu kwa sababu ya walivyo dhulumu. Hakika bila ya shaka katika hayo ipo Ishara kwa watu wanao jua.⁵²

44 Baada ya hao akaambiwa: Ingia katika jumba la Sulaiman. Na uwanja wake wa ndani ulikuwa umesakafiwa kwa kiyoo, na chini yake maji, na samaki wakiogelea humo. Kupandisha nguo miundi yake ya miguu ikaonekana, kwa kuwa alidhania ni maji. Sulaiman akamwambia hicho ni kiyoo, basi yakamuathiri yale madhaahiri ya kilimwengu, na akaona kuwa ufalme wake yeye haufai chochote mbele ya ufalme wa Nabii Sulaiman. Akasema: Mola Mlezi! Hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu kwa kughurika na ufalme wangu na ukafiri wangu. Na sasa ninanyenyekea pamoja na Sulaiman kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye kuumba walimwengu wote na kuwalea na kuwasimamia.

45 Na tuliwapelekea Thamud ndugu yao Saleh kuwafunza wamuamini Mwenyezi Mungu pekee. Wao wakakimbilia kugombana na kukhitalifiana. Wakawa makundi mawili. Moja lenye kuamini, na moja la kikafiri.

46 Saleh akasema nao kuwanasihi: Enyi watu! Mbona mnauhimiza adhabu mlio ahidiwa kabla ya kutubu? Kwa nini hamwombi msamaha kwa Mola wenu Mlezi, mkamuamini Yeye kwa kutaraji akurehemuni?

47 Wakasema: Sisi tunakuona wewe na hao walio nawe ni wakorofi, ndio tukapatilizwa na ukame. Yeye akasema: Sababu za kheri na shari zinazo kuteremkieni bila ya shaka yoyote zinatoka kwa Mwenyezi Mungu. Bali nyinyi ni watu mnao pewa mitihani ya neema na nakama, ili mpatе kuamini.

48 Na waongozi wa shari kati yao walikuwa ni tisa, kazi yao ni kufisidi katika nchi kwa maoni yao na madai yao. Wala haukuwa mtindo wao kutenda jema lolote.

49 Wale washirikina wakaambizana wenyewe kwa wenyewe: Apishaneni kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwamba kwa yakini tutamshambulia yeye na ahali zake, na tutawauwa. Kisha tutamwambia jamaa yao wa damu kwamba sisi hatukayaona mauwaji yake wala ya ahali zake. Na hakika sisi ni wasema kweli kwa haya tuliyo yataja.

50 Walipanga kumuwa Saleh na ahali zake, na Mwenyezi Mungu nyuma yao kapanga kumwokoia Nabii wake na ahali zake, na kuwateketeza wao, na hali wao hata hawatambui.

51 Ewe Nabii! Hebu tazama vipi yalikuwa matokeo ya mipango yao na mipango yetu. Sisi tuliwaangamiza wote hao wao na kaumu yao.

52 Na hebu yatazame mabaki yao. Utakuta nyumba zao zimeanguka, zimevurugika, kwa sababu ya udhalimu wao na kufu zao, na kumtakia shari Nabii wao. Hakika kwa walio fanyiwa kina Thamud ipo Ishara kwa watu wanao ujua uwezo wetu na wakawaidhika.

53. Na tukawaokoa wale walio amini na walio kuwa wanamchamngu.⁵³
54. Na Lut'i alipo waambia watu wake: Je! Mnafanya uchafu nanyi mnaona?⁵⁴
55. Hivyo nyinyi mnawaingilia wanaume kwa matamanio badala ya wanawake? Hakika nyinyi ni watu mnao fanya ujinga kabisa!⁵⁵
56. Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila ni kusema: Wafukuzeni wafwasi wa Lut'i katika mji wenu. Hao ni watu wanao jitia usafi.⁵⁶
57. Basi tukamwokoa yeye na ahali zake, isipo kuwa mkewe; tukamkadiria katika walio baki nyuma.⁵⁷
58. Na tukawanyeshea mvua. Ni ovu kweli kweli hiyo mvua ya walio kwisha onywa.⁵⁸
59. Sema: *Alhamdu Lillahi!* Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu! Na amani ishuke juu ya waja wake alio wateuwa. Je! Mwenyezi Mungu ni bora, au wale wanao washirikisha naye?⁵⁹
60. AU NANI yule aliye ziumba mbingu na ardhi, na akakuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo tukaziotisha bustani zenye kupendeza? Nyinyi hamna uwezo wa kuiotesha miti yake. Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali hao ni watu walio potoka.⁶⁰
61. Au nani yule aliye ifanya ardhi mahali pa kutua, na akajaalia ndani yake mito, na akaweka milima? Na akaweka baina ya bahari mbili kiziwizi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali wengi wao hawajui.⁶¹

53 Na Sisi tukakiokoa kikundi kilicho muamini Saleh kutokana na hilaki hii, na wakawa wanao gopa kuziacha amri zake.

54 Ewe Nabii! Mtaje Lut'i na khabari zake pamoja na kaumu ya watendao uchafu, pale alipo waambia: Je! Mnafanya dhambi hizi ambazo zimepita hadi ya uchafu na kinyume na maumbile, na hali nyinyi mnaona na mnaangalia uovu wa haya mliyo yashikilia?

55 Hivyo inaelekea katika nadhari ya akili zenu na maumbile kuwaingilia wanaume kwa matamanio yenu, na mkwawacha wanawake? Ama kweli nyinyi mmesibiwa na upumbavu na ujinga wa kufudikiza, hata imekuwa hamwezi tena kuteuwa baina ya kiovu na chema.

56 Haikuwa jawabu ya watu wake alipo wakataza ila ni kusema: Mtoleeni mbali Lut'i na wafwasi wake katika mji huu. Kwani wao wanajitakasa hawataki kushirikiana nasi katika haya tuyatendayo.

57 Basi Sisi tukamwokoa yeye na ahali zake na ile adhabu walio pelekewa wale watu, isipo kuwa mkewe. Mwenyezi Mungu alimkadiria awe na walio baki nyuma ili apate kuangamia kwa adhabu pamoja na makafiri.

58 Na Sisi tukawanyeshea mvua hao mafisadi, mvua ya adhabu na nakama. Ilikuwa mvua ya kuwahiliki walio onywa kuwa watapata adhabu chungu, na wala wasisikie.

59 Ewe Mtume! Sema: Hakika mimi namhimidi Mwenyezi Mungu na namsifu Yeye peke yake. Na namwomba Mwenyezi Mungu salama na maamkio kwa waja wake alio wateuwa kwa kuwapa Ujumbe wake. Na ewe Mtume! Waambie washirikina: Je! Kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja, Aliye Mpweke, ni bora kwa mwenye kuamini, au kuabudu masanamu mnayo mshirikisha naye, nayo hayawezi kukudhuruni wala kukufaeni?

60 Bali, ewe Mtume, waulize: Ni nani aliye ziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yake, na akakuteremshieni kutoka mbinguni mvua yenye manufaa, na kwa hiyo akakuotesheeni bustani nzuri zenye kupendeza. Msingeli weza nyinyi kuiotesha miti yake ya namna mbali mbali, na rangi mbali mbali, na matunda mbali mbali! Mipango hii iliyo umana sawa katika uumbaji inathibitisha kuwa hapana mungu pamoja na Mwenyezi Mungu. Lakini makafiri ni watu walio potoka wakaiaicha Haki na Imani, na wameelekea kwenye upotovu na ushirikina.

61 Bali waulize, ewe Mtume: Nani aliye itengeneza ardhi hata ikafaa kukaliwa na watu wakatulia humo, na akaumba mito kati yake, na juu yake akaumba milima kuizuilia isiyumbe yumbe, na akayatenganisha maji matamu na maji ya chumvi hata yasichanganyike? Hapana mungu pamoja na Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mwenye kuumba peke yake. Lakini wengi wa watu hawanafiki na ujuzi wa Haki kama ilivyo. Wamekuwa kama kwamba hawajui kitu.

62. Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na akaiondoa dhiki, na akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayo yazingatia.⁶²
63. Au nani yule anaye kuongoeni katika giza la bara na bahari, na akazipeleka pepo kuleta bishara kabla ya rehema zake? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ametukuka Mwenyezi Mungu juu ya wanao washirikisha naye.⁶³
64. Au nani anaye uanzisha uumbaji, kisha akaurejesha? Na nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.⁶⁴
65. Sema: Hapana katika mbingu na ardhi ajuaye ya ghaibu isipo kuwa Mwenyezi Mungu. Wala wao hawajui lini watafufuliwa.⁶⁵
66. Kwani huo ujuzi wao umefikilia kuijua Akhera? Bali wao wamo katika shaka nayo tu, bali wao ni vipofu nayo.⁶⁶
67. Na wakasema walio kufuru: Tutapo kuwa mchanga, sisi na baba zetu, hivyo kweli tutakuja tolewa?⁶⁷
68. Haya haya tuliahidiwa sisi na baba zetu zamani. Hayakuwa haya ila ni hadithi za uwongo za watu wa kale.⁶⁸
69. Sema: Nendeni katika ardhi, na tazameni ulikuwaje mwisho wa wakosefu.⁶⁹
70. Wala usiwahuzunukie wala usiwe katika dhiki kwa sababu ya hila zao wanazo zifanya.⁷⁰

62 Bali waulize, ewe Mtume: Nani anaye muitikia aliye shikwa na shida katika maombi yake, pale anapo shikwa na shida, akamtegemea Mwenyezi Mungu kwa unyonge na unyenyekevu, naye akamwondolea huyo mtu karaha iliyo msibu, na akakufanyeni warithi wa walio kutangulieni katika nchi? Hapana mungu pamoja na Mwenyezi Mungu wa kukupeni neema zote hizi. Lakini nyinyi makafiri, ni kuchache kabisa kuwaidhika kwenu.

63 Bali waulize, ewe Mtume: Nani anaye waongoza katika nyendo za katika giza la usiku katika safari za nchi kavu na baharini? Na nani anaye zipeleka pepo zinazo bashiria mvua, nayo ni rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu anaye fanya hayo? Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ametakasika kuwa na mshirika

64 Bali waulize, ewe Mtume: Nani anaye anzisha uumbaji tangu mwanzo, na kisha baada ya kupotea kwake akaurejesha kama ulivyo kuwa? Na nani anaye kuteremshieni riziki kutoka mbinguni, na akaitoa kwenye ardhi? Hakuna mungu pamoja na Mwenyezi Mungu atendaye hayo. Sema, ewe Mtume, kuwatahayarisha na kuwakanya: Kama nyinyi mnaye mungu asiye kuwa Mwenyezi Mungu basi tupeni hoja ya hayo, ikiwa mnadai kuwa nyinyi ni wasema kweli. Na wala hayataweza kuwa hayo kwenu.

65 Sema, ewe Mtume: Hakika mwenye kutenda yote haya peke yake ndiye Yeye *Subhanahu* aliye tengeka peke yake kwa kuyajua mambo ya ghaibu yalioko mbinguni na duniani. Na Yeye huyo ndiye Mwenyezi Mungu wa pekee. Wala watu hawajui wakati gani watafufuliwa kutoka makaburini kwao kwa ajili ya kuhisabiwa na kulipwa.

66 Ujuzi wao wa Akhera umefuatana na ujinga, na huo ukawapelekea kuitilia shaka. Nao wamekuwa vipofu hawaitambui Haki katika jambo lolote, kwa sababu upotovu umefisidi fahamu zao.

67 Wakasema makafiri kwa kukanya kufufuliwa: Hivyo sisi tukisha kuwa mchanga, na ikisha oza miili yetu na ya baba zetu walio tutangulia, ndio tutarejeshwa tutolewe upya tuwe wahai?

68 Muhammad ametuahidi kuwa tutafuliwa, kama Mitume walio tangulia walivyo waahidi baba zetu. Ingeli kuwa hayo ni kweli, basi yangeli kwisha kuwa. Haya si chochote ila ni uwongo tu wa watu wa kale.

69 Ewe Mtume! Waambie: Tembeeni duniani, na mtazame mabaki ya yaliyo wapata walio kadhibisha, nayo ni adhabu ya Mwenyezi Mungu. Huenda labda mkayazingatia haya, na mkaikhofu adhabu ya Akhera.

70 Ewe Mtume! Usiwahuzunukie makafiri wasio kufuata. Kwani kwa hakika waajibu wako ni kufikisha Ujumbe tu. Wala usiwe na dhiki kifuani mwako kwa sababu ya hila zao na vitimbi vyao. Kwani hakika Mwenyezi Mungu atakupa ushindi juu yao.

71. Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa mnasema kweli?⁷¹
72. Sema: Asaa ni karibu kukufikieni sehemu ya yale mnayo yahimiza.⁷²
73. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye fadhila kwa watu, lakini wengi wao hawashukuru.⁷³
74. Na hakika Mola wako Mlezi anayajua yanayo ficha vifua vyao na wanayo yatangaza.⁷⁴
75. Na hakuna siri katika mbingu na ardhi ila imo katika Kitabu kinacho bainisha.⁷⁵
76. Hakika Qur'ani hii inawasimulia Wana wa Israili mengi wanayo khitalifiana nayo.⁷⁶
77. Nayo hakika ni Uwongofu na Rehema kwa Waumini.⁷⁷
78. Hakika Mola wako Mlezi atawahukumu kwa hukumu yake, naye ni Mwenye nguvu Mjuzi.⁷⁸
79. Basi mtegemee Mwenyezi Mungu; hakika wewe uko juu ya Haki iliyo wazi.⁷⁹
80. Kwa hakika wewe huwezi kuwafanya maiti wasikie, wala kuwafanya viziwi wasikie wito, wanapo kwisha geuka kwenda zao.⁸⁰
81. Wala huwezi kuwaongoa vipofu waache upotovu wao. Huwezi kuwafanya wasikie isipo kuwa wenye kuziamini Ishara zetu; na hao ndio wat' iifu.⁸¹
82. Na itapo waangukia kauli juu yao, tutawatolea mnyama katika ardhi atakaye wasemeza, ya kuwa watu walikuwa hawana na yakini na Ishara zetu.⁸²

71 Na makafiri wanafanya ukomo wa juhudi yao kukanusha, na wanahimiza adhabu kwa kusema: Lini, basi, itakuwa hiyo adhabu ambayo mnatutishia kuwa itakuja, ikiwa nyinyi mnasema kweli kuwa adhabu itawashukia wanao kanusha?

72 Ewe Mtume! Sema: Huenda ikakukuteni, na imekukaribieni baadhi ya adhabu mnayo ihmiza.

73 Na hakika Mwenyezi Mungu Mola wako Mlezi, ewe Mtume, ni Mwenye neema na hisani kwa watu wote. Na katika rehema zake ni kuakhirisha hiyo adhabu kwa hao wanao kadhibisha. Lakini watu wengi hawaelewi fadhila za Mwenyezi Mungu wala hawamshukuru.

74 Ewe Mtume! Hakika Mwenyezi Mungu, Mola wako Mlezi, hapana shaka anajua kila wanalo lificha na wanalo litangaza, ikiwa maneno au vitendo viovu. Naye atakuja walipa kwayo..

75 Na hapana kilicho fichikana cha ghaibu, na kiwe kidogo vipi au duni, mbinguni au katika ardhi ila Mwenyezi Mungu anakijua, na amekidhibiti katika Kitabu cha Haki kilioko kwake

76 Hakika Kitabu hiki alichu teremshiwa Muhammad kinawawekea wazi Wana wa Israili ukweli wa yaliyo kuja katika Taurati, katika mambo ya itikadi na hukumu na hadithi. Na kinawarudisha kwenye kweli katika mambo waliyo khitalifiana kwayo.

77 Hakika Kitabu hichi ni Uwongofu wa kuokoa watu wasipotee, na ni Rehema ya kuwakinga na adhabu wote wenye kukiamini.

78 Ewe Mtume! Hakika Mola wako Mlezi atawapambanua watu wote Siku ya Kiyama kwa uadilifu wake. Naye ndiye Mwenye nguvu za kushinda, basi hapana wa kuipinga hukumu yake. Yeye ni Mjuzi wa kila kitu, basi mbele yake kweli haiwezi kuchanganyika na uwongo.

79 Basi, ewe Mtume, mtegemezee mambo yako Mwenyezi Mungu, na shikilia wito wako kwa kuamini kuwa utashinda tu, kwa sababu wewe uko juu ya Haki iliyo wazi, na mapuuza ya makafiri kukupuuza wewe hakutakudhuru kitu.

80 Ewe Mtume! Hakika wewe huwezi kuwaongoa hao, kwani hao ni kama maiti kwa kuto tambua kitu, na kama viziwi kwa kutosikia. Basi hao hawako tayari kuusikia wito wako kwa vile walivyo shikilia kukupuuza.

81 Na wala huwezi kuwaongoa kwenye Haki wale ambao wamepofuka kuona kwao na kutambua kwao. Na huwezi kumfanya asikie ila mwenye kukubali kuziamini Ishara zetu. Hao ndio wenye kut'ii na wenye kuitikia.

82 . Na itapo karibia kutimia ahadi ya Mwenyezi Mungu kuileta Saa ya Kiyama na kuwateremshia makafiri adhabu, Mwenyezi Mungu atawatolea watu mnyama kwenye ardhi atakaye waambia miongoni mwa atakayo sema: Hakika makafiri walikuwa hawaiamini miujiza yetu yote, na pia Siku ya Mwisho. Na hayo waliyo kuwa wakiyakanusha sasa yamekwisha kuwa. Na hichi basi kitisho cha hiyo Saa na yanayo

83. Na Siku tutapo kusanya kutoka kila umma kundi katika wanao kadhibisha Ishara zetu, nao watagawanywa mafungu mafungu.⁸³
84. Hata watakapo fika, atasema (Mwenyezi Mungu): Je! Nyinyi si mlizikanusha Ishara zangu pasipo kuzijua vyema? Au mlikuwa mkifanya nini?⁸⁴
85. Na kauli itawaangukia juu yao kwa vile walivyo dhulumu. Basi hao hawatasema lolote.⁸⁵
86. Je! Hawaoni kwamba sisi tumeufanya usiku ili watulie, na mchana wa kuangaza. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanao amini.⁸⁶
87. Na Siku litapo pulizwa baragumu, watahangaika waliomo mbinguni na katika ardhi, ila amtakaye Mwenyezi Mungu. Na wote watamfikia nao ni wanyonge.⁸⁷
88. Na unaiona milima unaidhania imetulia; nayo inakwenda kama mwendo wa mawingu. Huo ndio ufundi wa Mwenyezi Mungu aliye tengeneza vilivyo kila kitu. Hakika Yeye anazo khabari za yote myatendayo.⁸⁸
89. Watakao kuja na mema, watapata bora kuliko hayo. Nao watasalimika na mahangaika ya Siku hiyo.⁸⁹
90. Na watakao kuja na uovu, basi zitasunukishwa nyuso zao Motoni. Je! Kwani mnalipwa isipo kuwa mliyo kuwa mkiyatenda?⁹⁰
91. Ama mimi nimeamrisha nimuabudu Mola Mlezi wa mji huu aliye ufanya ni mtakatifu; na ni vyake Yeye tu vitu vyote. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu, wenye kunyenyekea.⁹¹

fuatia! (*Tazama Maelezo 27:82*)

83 Na ewe Mtume! Kumbuka siku tutapo wakusanya kutoka kila kundi la wenye kukadhibisha Ishara zetu, nao ni hao waongozi wanao fuatwa. Basi hao watachungwa wawe mbele ya kaumu zao kuendea hisabu na malipo.

84 Na pale watakapo simama mbele ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya hisabu, atasema *Subhanahu* kuwaambia kwa kuwadhili na kuwabinya: Nyinyi mlizikadhibisha Ishara zangu zote, na mkazikataa bila ya kuzingatia wala kufahamu. Na khasa mlikuwa mkitenda nini nanyi hamkuumbwa kwa upuuzi?

85 Na adhabu itawateremkia kwa sababu ya kujidhulumu nafsi zao kwa ukafiri. Basi watakuwa hawawezi kujilinda wala kutaka udhuru.

86 Bila ya shaka wameshuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ameufanya usiku ili wapate kupumzika, na akaufanya mchana una mwangaza, wapate kushughulikia kutafuta maisha yao. Hakika katika hayo zipo dalili wazi za Uguu wa Mwenyezi Mungu, na Upweke wake, kwa watu wanao zingatia wakaamini.

87 Na taja, ewe Mtume, Siku atapo puliza Israfil baragumu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na watapo ingiwa kiwewe walioko katika mbingu na katika ardhi kwa kitisho cha mpulizo huo, isipo kuwa huyo ambaye Mwenyezi Mungu atamtuliza na akamhifadhi na kitisho. Na viumbe vyote watakuja kwa Mola wao Mlezi nao ni madhalili.

88 Na unaiona, ewe Mtume, milima na unadhani haitaharaki imetulia tu, lakini kwa hakika inakwenda mbio kama mawingu. Na haya ni katika undaji wa Mwenyezi Mungu aliye umbwa kila kitu na akakizua. Hakika Yeye, *Subhanahu*, ni Mwenye kutimia ujuzi wake kwa yote wayatendayo watu, ya ut'iifu na maasi. Naye atawalipa kwayo. (*Tazama Maelezo 27:88*)

89 Kila mwenye kuleta wema katika dunia, nayo ni Imani na usafi wa ut'iifu, atapata huko Akhera thawabu kubwa kabisa kwa ajili ya aliyo yatanguliza. Na wenye mema haya watasalimika na khofu na kufazaika Siku ya Kiyama.

90 Na kila mwenye kuleta uovu katika dunia - nao ni shirki na maasia - na akafa na hayo, basi malipo ya kundi hili ni kuwa Mwenyezi Mungu atawasukumiza juu ya nyuso zao katika Moto, na wataambiwa hapo kwa kuwatahayarisha: Hakika hii leo hamlipwi ila kwa sababu ya shirki yenu na maasi yenu.

91 Ewe Mtume! Waambie watu: Sikuamrisha nimuabudu yeyote isipo kuwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa mji wa Makka aliye utukuza, na akaufanya mtakatifu wenye amani, usio faa kumwagwa damu ndani yake, wala kuwindwa wanyama wake, wala kukatwa miti yake. Na vitu vyote viliomo ulimwenguni ni vya Mwenyezi Mungu kuvimiliki na kuvitawala, na mimi nimeamrisha niwe katika

92. Na niisome Qur’ani. Na mwenye kuongoka, basi ameongoka kwa faida ya nafsi yake; na aliye potea - basi sema: Hakika mimi ni miongoni mwa waonyaji.⁹²

93. Na sema: *Alhamdu Lillahi*, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu. Yeye atakuonyesheni Ishara zake, na mtazijua. Na Mola wako Mlezi si mwenye kughafilika na myatendayo.⁹³

wanao mnyenyekea Mwenyezi Mungu.

92 Na nimeamrisha nidumishe kuisoma Qur’ani, kwa ibada, na kuzingatia, na kuwaitia watu wafuate yaliomo humo. Basi mwenye kuongoka, akaiamini, na akakufuata wewe, basi kheri ya hayo na malipo yake ni kwa nafsi yake. Na mwenye kupotea asiifuate Haki, na asikufuate wewe, mwambie: Hakika mimi ni Mtume, naonya, na nafikisha Ujumbe tu.

93 Na sema, ewe Mtume: *Alhamdu Lillahi*, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu kwa neema ya Unabii na Uwongofu. Mwenyezi Mungu atakuonyesheni hapa duniani athari za uwezo wake, na Akhera atakuonyesheni ukweli wa aliyo kwambieni, na mtayajua vilivyo. Wala Mwenyezi Mungu hashindwi kukuhisabieni wala haghafiliki na vitendo vyenu.

Sura 28 - Al-Qasas

Utangulizi

SURA YA AL-QASAS ni ya 28 katika mpango wa Msahafu. Nayo ni Sura ya Makka. Aya zake ni thamanini na nane.

Imetaja kwa kufafanua yaliyo kwisha tajwa kabla yake kwa jumla katika mambo ya Musa a.s. tangu kuzaliwa kwake katika enzi ya Firauni. Na Firauni alikuwa akiwauwa watoto wanaume wa Bani Israili kwa kukhofu asije tokea Nabii miongoni mwao atakaye teketeza ufalme wake.

Kisha yakaelezwa yaliyo tokea kukhusu kulelewa kwake Musa katika nyumba ya Firauni, mpaka alipo itoka Misri kukimbiza roho yake kwenda Madiani katika nchi ya Shamu. Na tena akarejea na mkewe, binti wa Shuaibu a.s.

Kisha yakatajwa ya mazungumzo ya Mwenyezi Mungu na Musa, na kumteuwa yeye kwa kumpa Utume, na mambo yaliyo tokea yaliyo mkhusu Firauni na wachawi wake pamoja na Musa, mpaka Mwenyezi Mungu alipo mzamisha Firauni na jeshi lake. Na Musa na Wana wa Israili walio kuwa pamoja naye wakaokoka. Kisha yaliyo watokea Wana wa Israili pamoja na Musa na nduguye Harun. Na zimetajwa pia khabari za walio kadhibisha kama Qaaruni na makafiri wengine walio watangulia. Na kwa maelezo haya yaliyo kusanya khabari mbali mbali ndio Sura hii ikaitwa Surat al-Qas'as', yaani Sura ya Visa, au Hadithi.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. T' A SIN MIM, (T' .S.M.)¹
2. Hizi ni Aya za Kitabu kinacho bainisha.²
3. Tunakusomea khabari za Musa na Firauni kwa Haki kwa ajili ya watu wanao amini.³
4. Hakika Firauni alitakabari katika nchi, na akawagawa wananchi makundi mbali mbali. Akalidhoofisha taifa moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wanaume na akiwaacha watoto wao wanawake. Hakika yeye alikuwa katika mafisadi.⁴
5. Na tukataka kuwafadhili walio dhoofishwa katika nchi hiyo na kuwafanya wawe waongozi na kuwafanya ni warithi.⁵

1 T'a Sin Mim, harufi za kutamkwa kubainisha kuwa Qur'ani hii ni muujiza wa harufi hizi hizi za mazungumzo yenu, na ili kuwazindua wenye kusikia.

2 Ewe Mtume! Aya hizi tunazo kufunulia wewe ni Aya za Qur'ani yenye kubainisha kwa uwazi, yenye kudhihirisha Haki iwe mbali na uwongo, na halali iwe mbali na haramu, na itoe ahadi ya kulipwa thawabu, na kuhadharisha na adhabu.

3 Tunakusimulia baadhi ya khabari za Musa na Firauni kwa ukweli, ili wapate kuzizingatia Waumini.

4 Hakika Firauni alipandwa na kiburi, na akapita mipaka katika udhalimu wake, na akatakabari mno katika nchi ya Misri. Akawafanya watu wa nchi hiyo makundi makundi, akiwanyanyua baadhi yao na akiwadhalilisha wenginewe, na khasa aliwadhoofisha Wana wa Israili. Akawa anawachinja watoto wao wanaume na akiwabakisha wanawake. Kwa hakika huyo alikuwa ni katika walio pita hadi katika ujabari na ufisadi.

5 Na Mwenyezi Mungu akataka kuwafadhilisha alio wafanya wanyonge Firauni katika nchi, na awafanye ndio wa kuongoza katika njia za kheri, na awarithishe ufalme na madaraka ya nchi.

- 6.** Na kuwapa nguvu katika nchi, na kutokana na wao kuwaonyesha kina Firauni na Hamana na majeshi yao mambo yale waliyo kuwa wakiyaogopa.⁶
- 7.** Tulimfunulia mama yake Musa kwa kumwambia: Mnyonyeshe. Na utakapo mkhofia basi mtie mtoni, na usikhofu wala usihuzunike. Hakika Sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya miongoni mwa Mitume.⁷
- 8.** Basi wakamwokota watu wa Firauni, aje kuwa adui kwao na huzuni. Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye makosa.⁸
- 9.** Na mkewe Firauni alisema: Atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako. Msimuuwe! Huenda akatufaa, au tumpange kuwa mwenetu. Wala wao hawakutambua.⁹
- 10.** Na moyo wa mama yake Musa ukawa mtupu. Alikuwa karibu kumdhihirisha, ingeli kuwa hatukumtia nguvu moyo wake ili awe miongoni mwa Waumini.¹⁰
- 11.** Naye akamwambia dada yake Musa: Mfuatie. Basi naye akawa anamuangalia kwa mbali bila ya wao kujua.¹¹
- 12.** Na tukamjaalia awakatae wanyonyeshaji wote tangu mwanzo, mpaka dada yake akasema: Je! Nikuonyesheni watu wa nyumba watakao mlea kwa ajili yenu, nao pia watakuwa wema kwake?¹²
- 13.** Basi tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike. Na ajue ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli, lakini wengi wao hawajui.¹³
- 14.** Na Musa alipo fika utu-uzima baraabara, tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo

6 Na tuwathibitishie katika nchi, na wawe na pahali pao humo. Na tuwathibitishie Firauni na Hamana na majeshi yao yale waliyo kuwa wakiyakhofu, nayo ni kuondoka ufalme wake kwa mkono wa mwenye kuzaliwa katika Wana wa Israili.

7 Na Mwenyezi Mungu alimfahamisha mama yake Musa, alipo kuwa anamkhoa asichinjwe na Firauni kama alivyo kuwa akiwachinja watoto wanaume wa Bani Israili, kwamba amnyonyeshe kwa kituo na hatauliwa na Firauni. Ikiwa anaogopa asije kutambulikana amtie katika sanduku, na amtie katika mto wa Nile bila ya khofu wala huzuni. Kwani bila ya shaka Mwenyezi Mungu amedhamini kumhifadhi na kumrejeshea mwenyewe, na kumtuma kwa Wana wa Israili.

8 Watu wa Firauni wakamchukua, ili aliyo kadiria Mwenyezi Mungu yatimie, yaani Musa apate kuwa Mtume mwenye kuwapinga wao, na mwenye kuwaletea huzuni, kwa kuitoa kombo dini yao na kuishambulia dhulma yao. Hakika Firauni na Hamana na wasaidizi wao walikuwa ni watu wenye madhambi, walio pindukia mipaka katika ujeuri na uharibifu.

9 Mke wa Firauni alipo mwona mtoto alimwambia mumewe: Mtoto huyu atatuletea furaha mimi na wewe. Tumweke, tusimuuwe, kwa kutaraji kuwa atakuja tufaa kuendesha mambo yetu. Au tumfanye mwenetu wa kumlea. Na wao kumbe hawatambui aliyo mkadiria Mwenyezi Mungu.

10 Na mama yake Musa akawa hajitambui kwa dhiki iliyo muingia kwa kuwa mwanawe kaangukia mikononi mwa Firauni. Akawa anakurubia kujitambulisha kwamba yeye ndiye mama yake. Lau ingeli kuwa Mwenyezi Mungu hakuutia imara moyo wake kwa kusubiri, basi angeli tangaza kuwa huyo ni mwanawe, jinsi alivyo kuwa akimhurumia, na pia ili awe miongoni mwa Waumini wenye kutulia.

11 Yule mama akamwambia dada yake Musa: Mfuatie upate kujua khabari zake. Basi akawa anamwona kwa mbali na anatahadhari asitambulikane, na Firauni na watu wake wakawa hawajui kama yule ni dada yake.

12 Mwenyezi Mungu alimjaalia yule mtoto akatae ziwa la kila mnyonyeshaji kabla hawajamjia mama yake. Watu wa Firauni wakaingiwa na ghamu, na wakashughulishwa na hayo. Yule dada yake ndio akawaambia: Nikuongozeni kwenye ukoo utakao muangalia huyu mtoto, na kumnyonyesha, na kumlea, nao watamtazama vizuri?

13 Wakaukubali uwongozi wake, na Mwenyezi Mungu akamrudisha kwa mama yake, ili nafsi yake itue, na afurahi kwa kurudi kwake, wala asihuzunike kwa kuwa mbali naye, na ili azidi kujua ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyo mpa kuwa atamrudishia imetimia wala hayendi kinyume. Lakini watu wengi walikuwa hawajui kurudi Musa kwa mama yake, kwani hayo yote yalifichikana kwao.

tunavyo walipa walio wema.¹⁴

15. Na akaingia mjini wakati wa kughafilika wenyeji wake, na akakuta humo watu wawili wanapigana - mmoja ni katika wenzake, na mwengine katika maadui zake. Yule mwenzake alimtaka msaada kumpiga adui yake. Musa akampiga ngumi, akamuwa. Akasema: Hiki ni kitendo cha Shet'ani; hakika yeye ni adui, mpotezaji dhaahiri.¹⁵

16. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimejidhulumu nafsi yangu; basi nisamehe. Akamsamehe; hakika Yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.¹⁶

17. Akasema: Mola wangu Mlezi! Kwa ulivyo nineemesha, basi mimi sitakuwa kabisa msaidizi wa wakosefu.¹⁷

18. Akapambazukiwa mjini asubuhi naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Mara yule yule aliye mtaka msaada jana akawa anampigia kelele amsaidie. Musa akamwambia: Hakika wewe ni mgomvi kweli kweli.¹⁸

19. Basi alipo taka kumshika kwa nguvu yule aliye adui wao wote wawili, akasema: Ewe Musa! Unataka kuniuwa kama ulivyo muuwa mtu jana? Wewe hutaki ila kuwa jabari katika nchi, wala hutaki kuwa miongoni mwa wenye maslahi.¹⁹

20. Na akaja mtu kutoka mwisho wa mji akipiga mbio, akasema: Ewe Musa! Wakubwa wanashauriana kukuuwa. Basi toka! Hakika mimi ni katika wanao kupa nasaha.²⁰

21. Basi akatoka, naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Akasema: Mola wangu Mlezi! Niokoe na watu madhaalimu.²¹

22. Na alipo elekea upande wa Madyana alisema: Asaa Mola wangu Mlezi akaniongoa

14 Na Musa alipo kwisha kuwa mtu mzima, na akakamilika, Mwenyezi Mungu alimpa hikima na ilimu. Na hisani kama hii tuliyo mpa Musa na mama yake, tunawapa wema wote kwa ajili ya wema wao.

15 Musa akaingia mjini Misri wakati walipo kuwa watu wake wameghafilika. Akawakuta watu wawili wanapigana. Mmoja ni katika Wana wa Israili, na mwengine katika kaumu ya Firauni. Yule Muisraili akamtaka msaada kumpiga khasimu yake. Naye Musa akamsaidia. Akampiga konde yule khasimu, akamuwa bila ya kukusudia. Musa akajuta na akasema: Hakika mimi kuja kufanya kitendo hichi ni kazi ya Shetani. Hakika Shetani ni adui aliye wazi kwa uadui na kupoteza.

16 Musa akasema kwa kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu na majuto: Ewe Mola wangu Mlezi! Mimi nimejidhulumu nafsi yangu kwa niliyo yatenda. Basi nighufirie kitendo changu hichi. Mwenyezi Mungu akamuitikia ombi lake na akamsamehe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkuu wa kusamehe, Mkunjufu wa rehema.

17 Musa akasema kwa kunyenyekea: Ewe Mola wangu Mlezi! Kwa haki ya kunineemesha kwako kwa kunipa hikima, na ilimu, niwezeshe nitende kheri na yanayo faa. Ukiniwezesha hivyo basi kabisa sitakuwa msaidizi wa makafiri.

18 Kulipo pambazuka asubuhi Musa alikuwapo mjini, Misri, naye yumo katika khofu, akitaraji kufikiwa na madhara kutokana na watu kwa sababu vile alivyo muuwa Mmisri. Akamwona yule Muisraili aliye mtaka msaada jana, naye akamtaka msaada mara ya pili katika ugomvi na Mmisri mwengine. Musa akamkemea kwa kumwambia: Hakika wewe mtu matata mno, na dhaahiri wewe ni mpotovu. Unafanya yale yale uliyo yafanya jana, na unaniita tena nikusaidie!

19 Na Musa alipo taka kumtumilia nguvu Mmisri, ambaye ni adui wao wote wawili; kwa sababu ya uadui huu, yule mtu alidhani kuwa Musa atamuwa, basi akasema: Unataka kuniuwa kama ulivyo muuwa mtu jana? Wewe hutaki ila kuwa muasi tu katika nchi, wala hutaki kuwa miongoni wanao lingania maslahi na kheri.

20 Akaja mtu mmoja Muumini katika kaumu ya Firauni kutoka mwisho wa mji, ilipo enea khabari ya Musa kumuwa Mmisri. Yule mtu akamwambia Musa kwamba watu wanapanga kutaka kumuwa. Akamwambia: Toka mji, ukimbie usije ukauliwa! Hakika mimi ni katika wanao kupa nasaha.

21 Musa akautoka mji naye amejaa khofu wasije maadui wakamdhuru, akimnyenyekea Mwenyezi Mungu amwokoe na udhalimu wa makafiri.

njia iliyo sawa.²²

23. Na alipo yafikia maji ya Madyana alikuta umati wa watu wananywesha (wanyama wao), na akakuta karibu yao wanawake wawili wanawazuia wanyama wao. Akasema: Mna nini? Wakasema: Hatunyweshi sisi mpaka wamalize hao wachunga. Na baba yetu ni mzee sana.²³

24. Basi Musa akawanyweshea; kisha akarudi kivulini, na akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia.²⁴

25. Basi mmoja katika wale wanawake wawili akamjia, naye anaona haya. Akasema: Baba yangu anakwita akulipe ujira wa kutunyweshea. Basi alipo mjia na akamsimulia visa vyake, alisema: Usiogope; umekwisha okoka kwenye watu madhaalimu.²⁵

26. Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu.²⁶

27. Akasema: Mimi nataka kukuoza mmojawapo katika binti zangu hawa wawili kwa kunitumikia miaka minane. Ukitimiza kumi, khiari yako; lakini mimi sitaki kukutaabisha. Inshallah utanikuta miongoni mwa watu wema.²⁷

28. Musa akasema: Hayo yamekwisha kuwa baina yangu na wewe. Muda mmojawo nikiumaliza sitiwi ubayani. Na Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu ya haya tunayo yasema.²⁸

29. Basi alipo timiza muda wake na akasafiri na ahali zake, aliona moto upande wa Mlima T'uri. Akawaambia ahali zake: Ngojeni! Mimi nimeona moto, labda nitakuleteeni kutoka huko khabari au kijinga cha moto ili mpate kuota moto.²⁹

22 Alipo elekea Madyana, kijiji cha Shuaibu - kwa kuwa huko iko amani - alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu amwongoe njia ya kheri na ya kuokoka.

23 Alipo yafikia maji ya Madyana wanapo nyweshea maji alikuta karibu na kisima kundi la watu wengi mbali mbali wanawanywesha wanyama wao wa mifugo. Na pahali pa chini kuliko hapo pao akawakuta wanawake wawili wanawazuia kunywa maji kondoo na mbuzi wao. Musa akawaambia: Mbona mko mbali na maji? Wakajibu: Hatuwezi kusukumana, na wala hatunyweshi sisi mpaka hawa wachunga wamalize wao kunywesha. Na baba yetu ni mkongwe, hawezi kuchunga wala kunywesha wanyama.

24 Musa akajitolea kuwakhudumia akawanyweshea. Kisha akenda kuegemea mti akipumzika baada ya kuhangaika kule, naye akisema kwa unyenyekevu: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mwenye haja ya kheri yoyote na riziki yoyote utayo niletea.

25 Mmoja wa wale mabinti akaja na ujumbe kutoka kwa baba yake baada ya kwisha jua khabari za Musa na wao wale mabinti. Naye akaja na huku anaona haya. Akasema: Baba yangu anakwita ili akulipe ujira kwa ulivyo tunyweshea maji. Basi alipo kwenda kwake na akamsimulia kisa chake cha kutoka Misri, akasema yule mzazi wa mabinti: Usikhofu; umekwisha okoka kwa hao watu madhaalimu. Kwani Firauni hana madaraka juu yetu.

26 Mmoja wa wale mabinti alisema: Ewe baba yangu! Mchukue umpe kazi ya kuchunga kondoo na mbuzi na kuwasimamia kwa haja zao. Hakika huyu ni mbora wa kumuajiri kwa sababu ya nguvu zake na uaminifu wake.

27 Shuaibu a.s. akamwambia: Mimi nataka kukuoza mmoja wa hawa mabinti zangu kwa mahari ya kunifanyia kazi muda wa miaka minane. Ukitimiza kumi itakuwa ni khiari yako. Wala mimi sitaki kukulazimisha huo muda mrefu. Na Inshallah, Mwenyezi Mungu akipenda, utaniona mimi ni katika watu wema, wenye kwenda nawe kwa ihsani na kutimiza ahadi.

28 Musa akasema: Hayo uliyo niahidi ni sawa sawa baina yangu na wewe. Muda wowote katika huo nitakao kufanyia kazi itakuwa nimekutimizia ahadi yako. Wala mimi sitaki zaidi kuliko hayo. Na Mwenyezi Mungu ni shahidi kwa tunayo yasema.

29 Musa alipo timiza muda wake walio patana, na akawa mume wa binti wa yule aliye mpokea, na akawa anarudi Misri, aliona njiani mwake katika upande wa Mlima wa T'uri moto unawaka. Akawaambia walio kuwa pamoja naye: Kaeni hapa. Mimi nimeuona moto, nimefurahi nao katika giza hili. Nitawendea

- 30.** Basi alipo ufikia aliitwa kutoka ng'ambo ya bonde la kuliani katika eneo lilio barikiwa kutoka kwenye mti: Ewe Musa! Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.³⁰
- 31.** Na tupa chini fimbo yako. Basi alipo iona ikitikisika kama nyoka, akarudi nyuma wala hakutazama. (Akaambiwa): Ewe Musa! Njoo mbele wala usiogope. Hakika wewe ni miongoni mwa walio salimika.³¹
- 32.** Ingiza mkono wako kwenye mfuko wako, utatoka mweupe pasipo na ubaya. Na jiambatishie mkono wako ukihisi khofu. Basi hizi ni dalili mbili zitokazo kwa Mola wako Mlezi kumpelekea Firauni na wakuu wa umma wake. Hakika hao walikuwa watu mafasiki.³²
- 33.** Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nilimuuwa mtu katika wao, kwa hivyo naogopa wataniuwa.³³
- 34.** Na ndugu yangu Harun ni fasihi zaidi ulimi wake kuliko mimi. Basi mtume ende nami kunisaidia, ili anisadikishe. Hakika mimi nina khofu watanikadhibisha.³⁴
- 35.** (Mwenyezi Mungu) akasema: Tutautia nguvu mkono wako kwa nduguyo, na tutakupeni madaraka, hata wasikufikilieni. Kwa sababu ya Ishara zetu nyinyi na watakao kufuateni mtashinda.³⁵
- 36.** Basi alipo wafikia Musa na Ishara zetu, walisema: Haya si chochote ila ni uchawi ulio zuliwa. Na hatukuyasikia haya kwa baba zetu wa zamani.³⁶
- 37.** Na Musa akasema: Mola wangu Mlezi ni Mwenye kujua kabisa nani anaye kuja na uwongofu unao toka kwake, na nani atakaye kuwa na mwisho mwema wa makaazi. Hakika wenye kudhulumu hawatafanikiwa.³⁷

nikuleteeni khabari ya njia, au nipate kijinga cha moto mpate walau moto wa kuota kujilinda na baridi.

30 Musa alipo ufikia moto alio uona alisikia kutoka upande wa kulia kwenye mti wenye kumea katika eneo lilio barikiwa ubavuni mwa Mlima, wito wa juu ukisema: Ewe Musa! Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu ambaye hapana anaye stahiki kuabudiwa isipo kuwa Yeye, Mwenye kuumba viumbe vyote na ni Mwenye kuvilinda na kuvihifadhi na kuvilea.

31 Na akanadiwa: Tupa chini fimbo yako. Akaitupa chini. Mwenyezi Mungu akaigeuza ikawa nyoka. Musa alipo iona inakwenda kama nyoka alikhofu, na akakimbia kwa kufazaika. Akaambiwa: Ewe Musa! Njoo, unaitwa urejee pahala pako, wala usiogope. Kwani wewe ni katika walio hifadhiwa na kila cha kuchukiza.

32 Na uingize mkono wako kwenye uwazi wa nguo yako utatoka mweupe, bila ya ila wala maradhi. Na jiambatishie mkono wako ubavuni mwako katika nguo ukiwa una khofu. Wala usishituke kwa kuona fimbo imekuwa nyoka, na kuona mkono wako umekuwa mweupe. Kwani miujiza hii miwili inatokana na Mwenyezi Mungu ya kumkabili nayo Firauni na kaumu yake watapo ukabili Ujumbe wako kwa kuukadhibisha na hali wametoka kwenye ut'iifu wa Mwenyezi Mungu.

33 Musa akasema, kwa khofu na kuomba msaada: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimemuuwa mtu katika hao, na nina khofu watakuja niuwa kwa kisasi.

34 Na ndugu yangu, Harun, ni fasihi zaidi ulimi wake kuliko mimi. Basi mtume awe pamoja nami katika kufikisha Utume, kwani mimi nina khofu watanikanusha.

35 Mwenyezi Mungu akasema, kuitikia ombi lake: Tutakutia nguvu kwa kumtuma Harun. Na tutakupeni nyinyi wawili madaraka, na tutakuungeni mkono kwa miujiza. Kwa hivyo hawatoweza kukuvamieni. Na nyinyi wawili na walio kufuateni na wakaongoka kwa msaada wenu, mtakuwa wenye kuwashinda hawa makafiri

36 Musa alipo wakabili kwa wito wake ulio tiliwa nguvu na miujiza iliyo wazi, waliyakanusha waliyo yaona, na wakasema: Haya si chochote ila ni uchawi unao mzulia Mwenyezi Mungu. Na hatukupata kusikia haya unayo tuitia kwa baba zetu wa zamani walio tangulia.

37 Na Musa alisema kumjibu Firauni na kaumu yake: Mola wangu Mlezi anajua kwa hakika kuwa mimi nimeleta Ishara hizi zenye kuonyesha Haki na Uwongofu kutokana naye Yeye. Basi Yeye ndiye shahidi

38. Na Firauni akasema: Enyi waheshimiwa! Sijui kama mnaye mungu asiye kuwa mimi. Ewe Haman! Niwashie moto unichomee udongo, unijengee mnara nipate kumchungulia mungu wa Musa. Na hakika mimi namwona yeye ni katika waongo.³⁸

39. Na alipanda kiburi yeye na majeshi yake katika nchi bila ya haki, na wakadhania kuwa hawatarudishwa kwetu.³⁹

40. Basi tukamshika yeye na majeshi yake, na tukawatupa baharini. Basi hebu angalia ulikuwaje mwisho wa wenye kudhulumu?⁴⁰

41. Na tuliwafanya ni waongozi waitao kwenye Moto. Na Siku ya Kiyama hawatanusuriwa.⁴¹

42. Na tukawafuatishia laana katika dunia hii, na Siku ya Kiyama watakuwa miongoni mwa wanao chusha.⁴²

43. Na hakika bila ya shaka tulimpa Musa Kitabu baada ya kwisha ziangamiza kaumu za mwanzo, ili kiwafumbue macho watu, na kiwe uwongofu, na rehema, ili wapate kukumbuka.⁴³

44. Wala wewe hukuwa upande wa magharibi tulipo mpa Musa amri, wala hukuwa katika walio hudhuria.⁴⁴

45. Lakini Sisi tuliziumba kaumu, na ukawa mrefu umri juu yao. Wala hukuwa mkaazi na watu wa Madyana ukiwasomea Aya zetu. Lakini ni Sisi tulio kuwa tukiwatuma Mitume.⁴⁵

46. Wala hukuwa kando ya mlima tulipo nadi. Lakini ni rehema itokayo kwa Mola

wangu kwa haya, ikiwa nyinyi mnanikadhibisha. Na Yeye anajua kuwa mwisho mwema ni wetu sisi watu wa Haki. Hakika makafiri hawapati kheri.

38 Na Firauni alipo shindwa kuhojiana na Musa, na akaendelea na jeuri zake, alisema: Enyi wahishimiwa! Mimi sijui kama yupo mungu wenu mwengine wewe isipo kuwa mimi. Na akamuamrisha waziri wake Haman amchomee matufali, na amjengee mnara mrefu apande, ende kumtazama huyo mungu anaye mlingania Musa.

39 Firauni na majeshi yake wakaendelea wakifanya kiburi katika nchi ya Misri kwa upotovu. Na wakadhani kuwa kabisa hawato fufuliwa Akhera kwa ajili ya hisabu na malipo.

40 Tukamng'oa Firauni kwenye utawala wake, na tukawavutia taratibu yeye na majeshi yake mpaka baharini, na tukawazamisha na huku tunawatupia sababu ya dhulma yao. Basi zingatia, ewe Muhammad, na uwahadharishe watu wako watazame vipi unakuwa mwisho wa wenye kudhulumu katika dunia yao. Na hakika wewe ni mwenye kusaidiwa kupata ushindi juu yao.

41 Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: Na tukawafanya hao ni wenye kuitia watu kwenye ukafiri, ambao khatima yake ni Moto. Na Siku ya Kiyama hawampati wa kuwanusuru na kuwatoa kwenye adhabu.

42 Na tukawafanya katika dunia hii wenye kupata laana, yaani wenye kutolewa wasiipate rehema yetu; na Siku ya Kiyama watakuwa miongoni mwa walio angamizwa. Na yaliyo simuliwa katika Aya mbili hizi juu yao ni dalili ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.

43 Na kwa yakini Mwenyezi Mungu alimteremshia Musa Taurati, baada ya kuwahiliki wakanushao katika kaumu zilizo tangulia, ili iwe nuru ya nyoyo. Kwani nyoyo hizo zilikuwa gizani, hazijui Haki wala uwongozi mwema. Kwani hao walikuwa wakitangatanga tu katika upotovu, na hawajui njia ya kupatia rehema kwa mwenye kutenda kwa ajili yake, na wakawaidhika kwa yaliyomo katika hiyo Taurati, na wakakimbilia kuzifuata amri, na kuyaacha yaliyo katazwa.

44 Wala wewe Muhammad, hukuwa na Musa upande wa magharibi wa huo mlima, pale Mwenyezi Mungu alipo agana naye kumuamrisha Ujumbe. Wala hukuishi zama za Musa, wala hukushuhudia alipo fikisha Utume. Basi vipi hawa watu wako wanakanusha Utume wako na wewe unawasomea khabari za walio tangulia?

45 Na lakini Sisi tumeziumba kaumu nyingi katika vizazi vilivyo pitiwa na zama ndefu, hata wakasahau maagano yaliyo chukuliwa kwao. Na wewe, ewe Mtume, hukuwa mkaazi wa Madyana hata ndio uwasimulie watu wa Makka khabari zao. Lakini Sisi tumekutuma wewe, na tumekupa khabari zao kwa njia ya wahyi (Ufunuo).

wako Mlezi ili uwaonye watu wasio pata kufikiwa na mwonyaji kabla yako, huenda wakakumbuka.⁴⁶

47. Na usije kuwasibu msiba kwa iliyo yatanguliza mikono yao, wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Mbona hukututumia Mtume nasi, tukafuata Ishara zako, na tukawa miongoni mwa Waumini?⁴⁷

48. Ilipo wajia Haki kutoka kwetu walisema: Mbona hakupewa kama aliyo pewa Musa? Je! Kwani wao hawakuyakataa aliyo pewa Musa zamani? Walisema: Ni wachawi wawili wanasaidiana. Na wakasema: Hakika sisi tunawakataa wote.⁴⁸

49. Sema: Basi leteni Kitabu kinacho toka kwa Mwenyezi Mungu chenye kuongoka zaidi kuliko hivi viwili tukifuata, kama nyinyi mnasema kweli.⁴⁹

50. Na ikiwa hawakuitikii, basi jua kuwa wanafuata pumbao lao tu. Na nani aliye potea zaidi kumshinda anaye fuata pumbao lake bila ya uwongofu utokao kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu.⁵⁰

51. Na sasa kwa yakini tumewafikishia Neno ili wapate kukumbuka.⁵¹

52. Wale tulio wapa Kitabu kabla yake wanakiamini hiki.⁵²

53. Na wanapo somewa wanasema: Tunaiamini. Hakika hii ni Haki inayo toka kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa ni Waislamu, tulio nyenyekea.⁵³

54. Basi hao watapewa ujira wao mara mbili kwa walivyo vumilia, na wakaondoa ubaya kwa wema, na wakatoa katika tuliyo waruzuku.⁵⁴

46 Wala wewe, ewe Mtume, hukuwepo hapo kando ya mlima pale Mwenyezi Mungu alipo mwita Musa na akamteuwa kumpa Utume wake. Lakini Mwenyezi Mungu amekujavya haya kwa njia ya wahyi (ufunuo), kutokana na rehema yake kwako na kwa umma wako, wapate kufikisha hayo kwa kaumu ambayo haikupata kufikiwa na Mtume kabla yako wewe, ili wakumbuke.

47 Ingeli kuwa makafiri wanapo patwa na mateso kwa sababu ya ukafiri wao wakataka udhuru na wakadai wakisema: Ewe Mola wetu Mlezi! Mbona hukutuletea Mtume tukamuamini na tukaikubali miujiza yake nasi tukawa miongoni mwa Waumini, basi usinge kuwepo Ujumbe wa Mitume.

48 Na alipo ileta Mtume wa Mwenyezi Mungu Qur'ani kutokana na Mwenyezi Mungu, makafiri walisema: Laiti yeye angeli pewa miujiza ya kuonekana na kama aliyo pewa Musa, na Kitabu cha kuteremka mara moja kama Taurati! Na hali hao walimkataa Musa na Ishara zake, kama hivi leo wanavyo mkataa Muhammad na Kitabu chake, na wakasema: Sisi tunawakataa wote wawili. Basi kukataa ndiko kuliko pelekea kuikanya miujiza.

49 Ewe Mtume! Wambie: Ikiwa hamuiamini Taurati na Qur'ani basi leteni kitabu kingine kinacho toka kwa Mwenyezi Mungu kilicho na uwongofu bora kuliko hivyo, au kama hivyo, nami nikifuata pamoja nanyi, ikiwa nyinyi mnasema kweli katika hayo madai yenu kwamba tuliyo kuja nayo ni uchawi.

50 Na ikiwa hawaitikii wito wako kwa kuleta kitabu kiongofu zaidi, basi jua kuwa wamebanwa na hawakubakiliwa na hoja yoyote, na kwamba kwa hayo wanafuata pumbao zao tu. Na hapana aliye zidi kwa upotovu kuliko yule anaye fuata pumbao lake katika dini, bila ya uwongofu kutokana na Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu hamwafiki mwenye kuidhulumu nafsi yake kwa kufuata upotovu bila ya kuitafuta Haki.

51 Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu amewateremshia Qur'ani kwa utungo, baadhi yake ikifuatia baadhi kwa mujibu wa inavyo takikana na hikima, na kulingana na ahadi, na maonyo, na hadithi, na mazingatio, ili wapate kupima na kuyaamini yaliomo ndani yake.

52 Wale ambao tuliwateremshia Taurati na Injili kabla ya kuteremka Qur'ani, na wakaviamini vitabu hivyo viwili, na wakasadiki yaliyo tajwa humo juu ya khabari za Muhammad na Kitabu chake, hao wanamuamini Muhammad na Kitabu chake.

53 Na hao wakaisomewa Qur'ani hufanya haraka kutangaza Imani yao, na husema: Tumeyaamini hayo, kwani hayo ni Haki inayo toka kwa Mola wetu Mlezi; na sisi tulimjua Muhammad na Kitabu chake hata kabla ya kuteremka kwake, nasi tukanyenyekea kabla ya kusomwa kwake.

54 Hao ambao waliamini Qur'ani na yaliyo teremshwa kabla yake, watapewa malipo yao maradufu - kwa ajili ya kuvumilia kwao mateso yaliyo wapata kwa ajili ya Imani, na wakakhiari vitendo vyema, na

55. Na wanapo sikia upuuzi hujitenga nao na husema: Sisi tuna vitendo vyetu, na nyinyi mna vitendo vyenu. *Salamun Alaikum*, Amani juu yenu! Sisi hatutaki kujibizana na wajinga.⁵⁵

56. Kwa hakika wewe humwongoi umpendaye, lakini Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye. Na Yeye ndiye anawajua zaidi waongokao.⁵⁶

57. Na wakasema: Tukiufuata uwongofu huu pamoja nawe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu. Je! Kwani Sisi hatukuwaweka imara katika pahala patakatifu, penye amani, ambapo huletewa matunda ya kila aina kuwa ni riziki itokayo kwetu? Lakini wengi wao hawajui.⁵⁷

58. Na miji mingapi iliyo jifakharisha tumeiangamiza! Na hayo maskani yao hayakukaliwa tena baada yao, ila kwa uchache tu. Na Sisi ndio tumekuwa warithi wao.⁵⁸

59. Na Mola wako Mlezi haangamizi miji mpaka ampeleke Mtume katika miji yake mikuu awasomee Ishara zetu. Wala hatuiangamizi miji mpaka watu wake wawe madhaalimu.⁵⁹

60. Na chochote mlichu pewa ni matumizi ya maisha ya dunia na pambo lake. Na yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ndio bora na yatakayo baki zaidi. Basi je, hamfahamu?⁶⁰

61. Je! Yule tuliye muahidi ahadi nzuri, tena naye akayapata, ni kama tuliye mstarehesha kwa starehe za maisha ya duniani, na kisha Siku ya Kiyama akawa miongoni mwa wanao hudhurishwa?⁶¹

wakayakabili maovu kwa kusamehe na ihsani, na wakatoa katika njia ya kheri kutokana na mali aliyo wapa Mwenyezi Mungu.

55 Na wanapo sikia upotovu wa wajinga hujitenga mbali nao, kwa kujiepusha na kuondoka, na husema: Sisi tuna a'mali yetu na hatuiachi, na nyinyi mna a'mali yenu ya upotovu na madhambi yake yapo juu yenu. Na sisi tunakuacheni na mambo yenu, kwani sisi hatupendi kusuhubiana na mahaahili.

56 Ewe Mtume! Hakika wewe una pupa sana kutaka hawa watu wako waongoke. Lakini wewe huwezi kumingiza katika Uislamu kila umpendaye. Lakini Mwenyezi Mungu humwongoa kuendea Imani yule anaye mjua kuwa ameelekea uwongofu na ameuhiari. Na Yeye ndiye Mwenye kujua, wala hapana ajuaye zaidi kuliko Yeye, nani atakaye ingia katika safu za wenye kuongoka.

57 Na washirikina wa Makka walimwambia Mtume s.a.w. kwa kujitolea udhuru kwa kubakia kwao katika dini yao: Tukikufuata wewe katika dini yako Waarabu watatutoa katika nchi yetu, na watatuhinda katika utawala wetu. Na hakika wao ni waongo katika kutoa udhuru wao huo. Kwani Mwenyezi Mungu alikuwa kawaweka imara na madhubuti katika nchi yao. Na akaifanya nchi takatifu yenye amani, hawashambuliwi wala hawauwawi, na hali wao ni makafiri. Na wanaletewa matunda na kheri nyengine za aina nyingi, ambazo Mwenyezi Mungu anawaletea kutoka kila upande. Basi huwaje awaondolee amani, na awaachilie wakinyakuliwa wakiongeza juu ya utakatifu wa Nyumba ya Alkaaba Imani kumuamini Muhammad! Lakini wengi wao hawajui Haki. Lau kuwa wanajua wasinge khofu kunyakuliwa.

58 Watu hawa hawazingatii yaliyo wapata kaumu zilizo kwisha tangulia. Iliangamizwa miji ya walio ghurika na neema za Mwenyezi Mungu, na kisha wakazikanusha na wakamkanusha Mwenyezi Mungu. Na haya majumba yao yamekuwa matupu, magofu, hayafai kukaliwa ila nadra tu kwa wapita njia. Na yamebaki hayana mwenye kuyamiliki baada yao ila Mwenyezi Mungu Mwenye utukufu na ukarimu.

59 Na haikuwa katika hikima ya Mwenyezi Mungu Mtukufu - naye ndiye Mola wako Mlezi aliye kuumba na kukuteuwa - kuiangamiza miji mikubwa ila baada ya kuwapelekea watu wake Mtume mwenye miujiza iliyo wazi awasomee Kitabu kilicho teremshwa, na awabainishie sharia, na kisha wawe hwaamini. Wala Sisi hatuangamizi miji mikubwa ila wakiwa watu wake wanaendelea na udhalimu na uadui.

60 Na kila kitu mlichu ruzukiwa katika starehe za dunia na mapambo yake kina ukomo wake kwa muda mfupi. Hayo yasikuziueni kuamini na kutenda vitendo vyema. Kwani hakika yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu huko Akhera, nayo ni thawabu na neema za milele, yana nafuu zaidi, na yana dawamu kuliko hayo yote. Basi kwa nini hamtumii akili zenu badala ya pumbao zenu?

61 Hawi sawa mwenye kuamini na akatenda mema na akastahiki ahadi ya Mwenyezi Mungu na ahadi

62. Na siku atakapo waita na akasema: Wako wapi mlio kuwa mkidai kuwa ni washirika wangu?⁶²
63. Watasema wale iliyo thibiti juu yao kauli: Mola wetu Mlezi! Hawa ndio tulio wapoteza. Tuliwapoteza kama tulivyo potea sisi. Tunajitenga nao mbele yako. Hawakuwa wakituabudu sisi.⁶³
64. Na itasemwa: Waiteni hao miungu wa kishirikina wenu! Basi watawaita, lakini hawatawaitikia, na wataiona adhabu; laiti wangeliki kuwa wameongoka!⁶⁴
65. Na siku atapo waita na akasema: Mliwajibu nini Mitume?⁶⁵
66. Basi zitawapotea khabari siku hiyo, nao hawataulizana.⁶⁶
67. Ama mwenye kutubu na akaamini na akatenda mema, huyo atakuwa miongoni mwa wenye kufanikiwa.⁶⁷
68. Na Mola wako Mlezi huumba na huteuwa atakavyo. Viumbe hawana khiari. Mwenyezi Mungu ametukuka na ametakasika na hao wanao washirikisha naye.⁶⁸
69. Na Mola wako Mlezi anayajua yaliyo ficha vifua vyao, na wanayo yatangaza.⁶⁹
70. Naye ni Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye. Sifa zote njema ni zake Yeye, mwanzo na mwisho. Na hukumu ni yake Yeye. Na kwake Yeye mtarejeshwa.⁷⁰

ya malipo mema na Pepo, na akayapata kama alivyo muahidi Mwenyezi Mungu; kulingana huyu na yule aliye kanusha na akatenda vitendo viovu, na yakamzuga maisha ya dunia na mapambo yake, na kisha Siku ya Kiyama akawa katika walio hudhurishwa kwa ajili ya hisabu, na akawa katika wenye kuhiliki kwa adhabu.

62 Ewe Mtume! Kumbuka siku watapo simama hawa mbele ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuhisabiwa, naye *Subhanahu* akawaita kwa kuwataharisha: Wako wapi hao miungu mlio dai kuwa ni washirika wangu, wapate kukuteteeni na kukuombeeni?

63 Watasema waongozi wa makafiri katika walio stahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na vitisho vyake: Ewe Mola wetu Mlezi! Hawa tulio waita kwenye shiriki na tukawapambia upotovu tuliwapoteza. Kwa sababu wao walikhiari ukafiri na wakaupokea, kama sisi tulivyo ukhiari na tukaupokea. Leo sisi tunajitenga nao kwako na ukafiri walio ukhiari duniani. Hawakuwa wao wakituabudu sisi; bali wakiabudu pumbao zao, na wakit'ii matamano yao

64 Na Mwenyezi Mungu kuwaamrisha makafiri ni kwa kuwataharisha tu, kwa vile kuwataka wawaita wale miungu ya ushirikina wawaokoe na adhabu yake, kama walivyo dai. Wakaitikia kwa unyonge, na wakawaita kwa kuwa hawana hila. Wasipate jawabu yoyote. Wakaiona adhabu walio ahidiwa iko mbele yao, na wakatamani lau kuwa katika dunia yao wangeliki kuwa Waumini walio ongoka, jinsi ya adhabu iliyo wafikia.

65 Na ewe Mtume! Taja vile siku washirikina watapo itwa na Mwenyezi Mungu kwa kutahayarishwa, na wakaambiwa: Mliwajibu nini Mitume wangu nilio watumu kwenu wakuiteni kwenye Imani, nao wakafikisha Ujumbe?

66 Khabari hizo zikawapita hawazitambui kama kwamba ni vipofu. Ikawa hapana amuulizae mwenziwe, kwani wote walikuwa sawa sawa wameshindwa kujibu.

67 Hii ndiyo hali ya washirikina. Ama mwenye kutubu kutokana na shiriki yake, na akaamini Imani ya kweli, na akatenda mema, basi huyo hutaraji kuwa kwa Mwenyezi Mungu miongoni mwa walio fuzu kuipata radhi ya Mwenyezi Mungu, na neema ya kudumu yenye kuendelea milele.

68 Na Mola wako Mlezi anaumba atakalo kwa uwezo wake. Na anamkhitari amtakaye kwa hikima yake kumpa Ujumbe na ut'iifu kwa kujua kwake mwenyewe kufaa kwao. Wala hawawezi viumbe, na wala si haki, kumchagulia Mwenyezi Mungu walitakalo katika dini potovu, na miungu ya uwongo. Mtukufu ametakasika shani yake na washirika.

69 Ewe Mtume! Mola wako Mlezi anajua baraabara yaliomo katika vifua vya washirikina ya uadui wao juu yako, na wanayo tangaza kwa ndimi zao ya kukushutumu na kukupinga kwa ulivyo teuliwa kupewa Utume.

70 Na Mola wako Mlezi, ewe Mtume, ndiye Mwenyezi Mungu wa Haki, ndiye pekee Mwenye Ungu, Mwenye kustahiki pekee yake kuhimidiwa na waja wake katika dunia kwa neema zake na uwongofu wake,

- 71.** Sema: Mwaonaje, Mwenyezi Mungu angeli ufanya usiku umekukalieni moja kwa moja mpaka Siku ya Kiyama, mungu gani asiye kuwa Mwenyezi Mungu atakaye kuleteeni mwangaza? Basi je, hamsikii?⁷¹
- 72.** Sema: Mwaonaje, Mwenyezi Mungu angeli ufanya mchana umekukalieni moja kwa moja mpaka Siku ya Kiyama, mungu gani asiye kuwa Mwenyezi Mungu ataye kuleteeni usiku mkapumzika humo? Basi je, hamwoni?⁷²
- 73.** Na ni katika rehema zake amekufanyieni usiku na mchana mpate kupumzika humo na mtafute fadhila zake, na ili mpate kushukuru.⁷³
- 74.** Na siku atakapo waita na akasema: Wako wapi hao mlio kuwa mkidai kuwa ni washirika wangu?⁷⁴
- 75.** Na tutatoa shahidi katika kila umma, na tutasema: Leteni hoja zenu! Hapo watajua kwamba hakika kweli ni ya Mwenyezi Mungu, na yatawapotea yale waliyo kuwa wakiyazua.⁷⁵
- 76.** Hakika Qaruni alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia dhulma. Na tulimpa khazina ambazo funguo zake zinawatopeza watu wenye nguvu kuzichukua. Walipo mwambia watu wake: Usijigambe! Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanao jigamba.⁷⁶
- 77.** Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanya

na katika Akhera kwa uadilifu wake na kulipa kwake. Na Yeye peke yake ndiye Mwenye hukumu, na kuamua baina ya waja wake. Na kwake Yeye ndiyo marejeo ya kwendea.

71 Ewe Mtume! Sema: Enyi watu! Niambieni, Mwenyezi Mungu akikufanyieni usiku uendelee mfululizo bila ya mchana mpaka Siku ya Kiyama, je! Mnaye yeyote asiye kuwa Mwenyezi Mungu wa kukuleteeni mchana wenye mwangaza mkaweza kushughulikia maisha yenu na kuendesha mambo yenu ya dunia? Hamna hayo nyinyi. Basi kwa nini hamsikii kwa sikio la kuwaza na kuzingatia?

72 Ewe Mtume! Waambie watu: Mwenyezi Mungu akikujaalieni mchana mfululizo bila ya usiku mpaka Siku ya Kiyama, yupo asiye kuwa Mwenyezi Mungu wa kukuleteeni usiku mkapata kupumzika na kazi za mchana? Hamna hayo nyinyi. Basi kwa nini hamzioni Ishara za Mwenyezi Mungu, mkaamini na mkaongoka?

73 Na miongoni mwa rehema za Mwenyezi Mungu kwa viumbe vyake ni kuwa kawaambia usiku na mchana, inayo fuatana, ili wapate kupumzika usiku, na washughulikie kutafuta riziki zao na manufaa yao mengine wakati wa mchana, na watambue fadhila za Mwenyezi Mungu juu yao wapate kumshukuru. (Tazama Maelezo 28:73)

74 Na pia, ewe Mtume, kumbuka siku watapo itwa washirikina na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa wito wa kuwataharisha, wakaambiwa: Wako wapi washirika ambao mkidai kuwa ni miungu wa kukunusuruni, au waombezi wa kukuombeeni?

75 Na Siku ya Kiyama tutatoa kutoka kila umma shahidi, naye ndiye Nabii wao, wa kutoa ushahidi dhidi yao kwa waliyo kuwa wakiyafanya duniani. Hapo Sisi tutawaambia wakhalifu miongoni mwao: Nini hoja yenu kwa mliyo kuwa mkiyatenda ya ushirikina na maasi? Watashindwa kujibu, na watajua hapo kuwa Haki yote iko kwa Mwenyezi Mungu, tangu mwanzo mpaka mwisho. Na yatapotea, kama vinavyo potea vitu vilio potea, yote waliyo kuwa wakimzulia Mwenyezi Mungu.

76 Sura hii inasimulia kisa cha Qaruni. Naye alikuwa katika kaumu ya Musa. Akapanda kiburi juu yao kwa kughurika kwa nafsi yake na mali yake. Na Mwenyezi Mungu alikuwa kampa khazina za mali mengi. Hata ikawa funguo zake tu zikiwaemea kundi la wanaume wenye nguvu! Na alipo ghurika na neema ya Mwenyezi Mungu juu yake, na akakufuru kwa sababu yake, watu walimpa nasaha, wakamwambia: Usidanganyike kwa mali yako, wala furaha kwa ajili yake isikusaliti hata ukaacha kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kwani hakika Mwenyezi Mungu hawapendi watu walio danganyika na wakasalitika. Na funzo la kisa hichi ni kuwa makafiri walio mkataa Muhammad s.a.w. walighurika na mali yao. Basi Qur'ani inawaelezea kuwa mali yao si chochote cha kutajika ukilinganisha na mali ya Qaruni.

wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi.⁷⁷

78. Akasema: Kwa hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyo nayo. Je! Hakujua kwamba Mwenyezi Mungu keshwa waangamiza, katika vizazi vya walio kabla yake, watu walio kuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye, na wenye makundi makubwa zaidi kuliko yake. Na wakosefu hawataulizwa khabari ya dhambi zao.⁷⁸

79. Basi akawatokea watu wake katika pambo lake. Wakasema wale walio kuwa wanataka maisha ya duniani: Laiti tungeli kuwa tunayo kama aliyo pewa Qaruni! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa.⁷⁹

80. Na wakasema wale walio pewa ilimu: Ole wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipo kuwa wenye subira.⁸⁰

81. Basi tukamdidimiza yeye na nyumba yake katika ardhi; wala halikuwepo kundi lolote la kumnusuru kwa Mwenyezi Mungu, wala hakuwa miongoni mwa wanao jitetea.⁸¹

82. Na wale walio tamani kuwa pahala pake jana, wakawa wanasema: Kumbe Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye katika waja wake, na humdhikisha amtakaye. Ingeli kuwa Mwenyezi Mungu hakutufanyia hisani angeli tudidimiza. Kumbe makafiri hawafanikiwi!⁸²

83. Hayo ndiyo makaazi ya Akhera, tumewafanyia wale wasio taka kujitukuza

77 Na katika utajiri na neema alizo kupa Mwenyezi Mungu toa fungu kwa ajili ya Njia ya Mwenyezi Mungu, na tenda a'mali kwa ajili ya makaazi ya Akhera. Na wala usiinyime nafsi yako fungu lake kwa matumizi ya halali katika dunia. Na wafanyie wema waja wa Mwenyezi Mungu, kama vile alivyo kufanyia wema wewe kwa neema zake. Wala usifanye uharibifu katika ardhi ukapita mipaka ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu *Subhanahu* hawafurahii mafisadi kwa vitendo vyao viovu

78 Basi Qaruni hakusikia nasaha ya watu wake, na akasahau fadhila ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yake. Na akajifanya hajui kwamba Mwenyezi Mungu alikwisha waangamiza wengi walio mzidi yeye sana katika uwezo na mazoezi ya kuchuma mali kwa njia mbali mbali za uchumi. Na wakosefu hawaulizwi madhambi yao, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anayajua. Basi wataingizwa Motoni bila ya hisabu. Kuulizwa kwao ni kwa ajili ya kutahayarishwa tu.

79 Na Qaruni hakujali nasaha za watu wake. Akawatokea naye kajipamba mapambo yake. Wakadanganyika naye wale walio kuwa wanapenda starehe za maisha ya dunia, na wakatamani nao wangeli kuwa nayo mali na hadhi kubwa ya maisha kama aliyo pewa Qaruni.

80 Ama wale ambao Mwenyezi Mungu amewaruzuku ilimu yenye manufaa hawakusalitika na hayo. Wakawaelekea walio danganyika kwa kuwanasihi wakiwaambia: Msiyatamani haya, wala msiiache Dini. Kwani yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ya thawabu na neema ni safi zaidi kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Na hiyo ni nasiha ya kweli ambayo hawaikubali ila wenye kuzipiga jihadi nafsi zao, na wakasubiri katika ut'iifu.

81 Mwenyezi Mungu akamdidimiza katika ardhi, na ardhi ikammeza yeye na nyumba yake na vyote vilio kuwemo ndani yake, mali na mapambo yake. Hakuwa na wasaidizi wa kumkinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na wala yeye mwenyewe hakuweza kujinusu nafsi yake.

82 Na wale walio kuwa karibuni wakikitamani cheo chake cha duniani, wakawa wanatamka maneno ya masikitiko na majuto baada ya kuyafikiri yaliyo msibu yeye. Wakawa wanasema: Hakika Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye katika waja wake Waumini na wasio kuwa Waumini. Na humdhikisha amtakaye katika hao. Na wakawa wanasema kwa kushukuru: Lau kuwa Mwenyezi Mungu hakutufanyia hisani kwa kutupa uwongofu tukafuata Imani, na akatuhifadhi tusiporonyoke angeli tutia katika mitihani kwa kutukubalia tuliyo kuwa tunayatamani, na akatufanyia kama alivyo mfanyia Qaruni. Hakika wanao ipinga neema ya Mwenyezi Mungu hawafanikiwi kwa kuokoka na adhabu yake.

dunianiwala ufisadi. Na mwisho mwema ni wa wachamngu.⁸³

84. Atakaye tenda wema atapata malipo bora kuliko huo wema alio utenda. Na atakaye tenda uovu, hawalipwi watendao uovu ila waliyo kuwa wakiyatenda.⁸⁴

85. Hakika aliye kulazimisha kuifuata Qur'ani hapana shaka atakurudisha pahala pa marejeo. Sema: Mola wangu Mlezi ndiye anaye mjua zaidi mwenye kuja na uwongofu, na nani aliyomo katika upotofu ulio dhaahiri.⁸⁵

86. Nawe hukuwa unataraji kuletewa Kitabu; lakini ni rehema tu ya Mola wako Mlezi. Basi usiwe msaidizi wa makafiri.⁸⁶

87. Wala wasikuzuie kuzifuata Aya za Mwenyezi Mungu baada ya kuteremshiwa wewe. Na lingania kwa Mola wako Mlezi, wala usiwe miongoni mwa washirikina.⁸⁷

88. Wala usimwombe pamoja na Mwenyezi Mungu mungu mwenginewe. Hapana mungu ila Yeye. Kila kitu kitaangamia isipo kuwa Yeye. Hukumu iko kwake, na kwake mtarejzwa.⁸⁸

83 Hayo ndio makaazi ambayo umesikia khabari zake, ewe Mtume, na zikakufikia sifa zake, nayo ni Pepo. Tumeiweka makhsusi kwa ajili ya Waumini wat'iifu, wasio taka kujipa ubora na utukufu wa kidunia, na wala hawapotoki kuendea ufisadi na maasi. Na mwisho mwema ni wa wale ambao nyoyo zao zimejaa khofu ya Mwenyezi Mungu, na wanatenda yanayo mridhisha Yeye.

84 Mwenye kuja na wema, nao ni Imani na vitendo vyema, atapata malipo marudufu kwa ajili yake. Na mwenye kuja na uovu, nao ni ukafiri na maasi, halipwi ila mfano wa vitendo vyake viovu.

85 Hakika Mwenyezi Mungu aliye kuteremshia Qur'ani na akakulazimisha uifikishe kwa watu na ushikane nayo hapana shaka atakurudisha kwenye miadi, nako ni Siku ya Kiyama, ili apambanue baina yako na wale wanao kukadhibisha. Ewe Mtume! Waambie makafiri: Mola wangu Mlezi ndiye anaye jua kwa ujuzi usio pikuliwa na yeyote, nani aliye mpa uwongofu na uwongozi, na nani aliye tumbukia katika upotovu unao tambulikana na kila mwenye akili nzima.

86 Ewe Mtume! Wewe hukuwa wewe ukitaraji na ukingojea uteremshiwe hii Qur'ani. Lakini Mwenyezi Mungu amekuteremshia kutoka kwake kwa kukurehemu wewe na umma wako. Basi ikumbuke neema hii, na shikilia kuifikisha. Wala usiwe wewe na wanao kufuata kuwa wasaidizi wa makafiri kwa wanayo yataka.

87 Wala makafiri wasikuachishe kuzifikisha Aya za Mwenyezi Mungu na kuzitenda, baada ya kwisha teremka wahyi (ufunuo) kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na ukawa ndio Ujumbe wako. Na shikilia Wito kuwaitia watu kwenye Dini ya Mwenyezi Mungu. Wala usiwe wewe wala wanao kufuata katika wasaidizi wa washirikina kwa kuwasaidia kwa wayatakayo.

88 Wala usimwabudu mungu yeyote isipo kuwa Mwenyezi Mungu tu. Kwani hapana kabisa mungu wa kuabudiwa kwa haki isipo kuwa Yeye. Kila kitu isipo kuwa Mwenyezi Mungu kitaangamia na kwisha. Wa kudumu milele ni Yeye Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye mwenye hukumu ya kutekeleza duniani na Akhera. Na kwake Yeye ndiyo yako marejeo ya viumbe vyote, hapana hivi wala hivi.

Sura 29 - Al-'Ankabut

Utangulizi

SURA HII NI ya Makka, na idadi ya Aya zake ni 69. Lakini Aya 1 mpaka 11 ziliteremka Madina. Sura hii imeanzia kwa kubainisha kwamba hapana budi ila Imani ya Waumini itiwe mitihanini kwa misukosuko na jihadi kwa ajili ya kulinda dola ya Haki na Imani. Na binaadamu ameusiwa kwa wazazi wake pamoja na amri ya jihadi, ili ukusanyike wema na jihadi, na baina ya watu wa namna mbali mbali na Imani. Na imeelezwa kwamba miongoni mwao yupo anaye sema kwa ulimi wake kwamba ameamini na hali moyo wake haukukubali. Kisha Sura hii imetaja khabari za Nuhu na kaumu yake, na kadhaalika imeeleza kisa cha Ibrahim katika wito wake. Na ikabainisha mafunzo hayo kwa ajili ya Mtume s.a.w. Kisha ikasimulia jawabu ya watu wa Ibrahim. Na ikaeleza khabari za Lut'i na kisa cha kaumu yake, na kuteremka kwa Wajumbe Malaika wa Mwenyezi Mungu kuja kuwahiliki, na wakaokoka ahali zake isipo kuwa mkewe. Kisha *Subhanahu* akaashiria kisa cha Shuaibu pamoja na Madyana, na cha Hud na A'di, na Saleh na Thamud, na kudanganyikiwa kwa Qaruni na Firauni na Hamani na matokeo ya mwisho wao. Na Yeye *Subhanahu* amebainisha kwamba kuabudu masanamu kwa washirikina kunategemea hoja iliyo kuwa dhaifu kabisa kuliko jumba la buibui. Na kwamba mifano kama hii hawaelewi ila wale wanao tumia akili zao. Na baada ya hayo Mwenyezi Mungu akamuamrisha Nabii wake asijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia nzuri. Na Yeye *Subhanahu* akaashiria kwamba Nabii s.a.w. hajui kusoma wala kuandika, na hayo yanazidi kuonyesha Utume wake. Na pia *Subhanahu* ametaja ukaidi wa washirikina katika kutaka kwao waletewe miujiza ya kuiona, nayo wataikataa kama walivyo ikataa kaumu ya Musa na wengineo. Na akagusia kule kuhimiza kwao kuteremshiwa adhabu. Naye amewabainishia adhabu itakayo wapata. Naye *Subhanahu* akataja malipo ya Waumini na Makafiri Siku ya Kiyama, na akataka watu watazame baada ya hayo ulimwengu na neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ziliomo ndani yake. Kisha akataja thamani ya uhai wa duniani ukilinganisha na wa Akhera, na hali ya washirikina katika unyonge wao na kumkimbilia kwao Mwenyezi Mungu wanapo kuwa katika khofu, na wanapo kuwa na nguvu na wakawa katika usalama wanavyo mshirikisha Mwenyezi Mungu. Kisha akaeleza neema zake anazo wapa katika Nyumba Takatifu ya Makka, na wanavyo zikanya neema hizo. Kisha Mwenyezi Mungu akabainisha fadhila za wanao pigana Jihadi.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Mim (A.L.M.)¹

2. Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema: Tumeamini. Naowasijaribiwe?²

1 Alif Lam Mim - Hizi ni harufi za kutamkwa na zikasikilizana, zilizo letwa ili kubainisha kwamba hii Qur'ani yenye kuwaemea watu kuiiga imetungwa kwa harufi hizi hizi mnazo ziweza kuzitamka vizuri. Na pia ni kwa ajili ya kuwazindua wasikilizaji na wapate kuiangalia Haki.

2 Hivyo watu wanadhani kwamba wataachiliwa tu hivi hivi kwa sababu ya kutamka kwao shahada mbili basi, bila ya kujaribiwa kwa mitihani na shida ili utambulikane ukweli wa Imani yao? La, sivyo hivyo!

3. Hakika tuliwajaribu walio kuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu atawatambulisha walio wa kweli na atawatambulisha walio waongo.³
4. Au wanadhani wanao tenda maovu kwamba watatushinda? Hukumu mbaya hiyo wanayo hukumu.⁴
5. Mwenye kutaraji kukutana na Mwenyezi Mungu, basi hakika miadi ya Mwenyezi Mungu itafika bila ya shaka. Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.⁵
6. Na anaye fanya juhudi basi bila ya shaka anafanya juhudi kwa ajili ya nafsi yake. Hakika Mwenyezi Mungu si mhitaji wa walimwengu.⁶
7. Na walio amini na wakatenda mema, kwa yakini tutawafutia makosa yao, na tutawalipa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.⁷
8. Na tumemuusia mwanaadamu kuwafanyia wema wazazi wake. Na ikiwa watakushikilia unishirikishe Mimi na usiyo kuwa na ujuzi nayo, basi usiwa'ii. Kwangu Mimi ndio marejeo yenu, na nitakwambieni mliyo kuwa mkiyatenda.⁸
9. Na walio amini na wakatenda mema, bila ya shaka tutawatia miongoni mwa watu wema.⁹
10. Na katika watu wapo wanao sema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu. Lakini wanapo pewa maudhi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wanayafanya mateso ya watu kama ni adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na inapo kuja nusura kutoka kwa Mola wako Mlezi husema: Hakika sisi tulikuwa pamoja nanyi. Kwani Mwenyezi Mungu hayajui yaliomo vifuani mwa walimwengu?¹⁰

Bali hapana budi kutiwa mitihanini.

3 Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu alikwisha ziharibu kaumu zilizo tangulia kwa kuwapa shida na namna mbali mbali za neema na mitihani, ili yapate kuonekana yale ambayo Yeye anayajua tangu mwanzo, na awatengue baina ya walio kuwa wakweli katika Imani yao, na waongo.

4 Wanadhani wanao mshirikisha Mwenyezi Mungu na wanamuasi kwamba watatuponyoka katika kukimbia kwao kuikimbia adhabu ya Mwenyezi Mungu na malipo yake? Kuhukumu kwao huku ni kuovu mno!

5 Mwenye kuamini kufufuliwa, na akawa anataraji malipo ya Mwenyezi Mungu, na anaikhofu adhabu yake, basi huyo Imani yake ni ya kweli. Basi na aingie kwenye vitendo vyema. Kwani Siku iliyo ahidiwa itakuja tu, hapana hivi wala hivi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia maneno ya waja, ni Mwenye kuvijua vitendo vyao. Na atamlipa kila mmoja kwa anavyo stahiki.

6 Na mwenye kuwania jihadi kwa sababu ya kutukuza Neno la Mwenyezi Mungu, na akapambana na nafsi yake ivumilie juu ya ut'iifu, basi malipo ya jihadi yake yatamrudia mwenyewe. Na hakika Mwenyezi Mungu aliye takasika si mhitaji wa ut'iifu wa walimwengu.

7 Na wale walio sifika kwa Imani na wakatenda mema hapana shaka tutawaondolea makosa yao, na tutawasamehe, na tutawalipa bora ya malipo kwa vitendo vyao vyema.

8 Na Mwenyezi Mungu amemuamrisha mwanaadamu afanye ukomo wa uwezo wake kuwafanyia wema wazazi wake na kuwat'ii. Na wakikushikilia kumfanyia shirki Mwenyezi Mungu - na hayo hayakubaliki katika ilimu wala akili - basi usiwa'ii. Na marejeo ya viumbe vyote ni kwa Mwenyezi Mungu, na Yeye atawaeleza walio yatenda duniani, na atawalipa kwayo.

9 Na walio msadiki Mwenyezi Mungu na Ujumbe wake, na wakatenda mema, basi hao hapana shaka Mwenyezi Mungu atawaingiza pamoja na walio wema, wapate malipo yao na wayastarehee.

10 Na miongoni mwa watu yupo ambaye husema kwa ulimi wake: Tumeamini. Na akipata dhiki yoyote kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hukereka na akafitinika hata katika dini yake. Wala haifikirii adhabu ya Mwenyezi Mungu ya Siku ya Kiyama. Yeye huyo huwa kama kwamba anafanya mateso ya wanaadamu kuwa sawa na adhabu ya Mwenyezi Mungu ya Akhera. Mwenyezi Mungu akiwanusuru Waumini, akawapa ushindi kuwashinda maadui zao na wakupata ngawira, watu hao wanao dhihirisha imani huja wakawaambia Waislamu: Sisi ni wenzenu katika Imani. Basi hebu tupeni nasi fungu letu la ngawira. Wasidhani watu hawa kwamba mambo yao yamefichikana kwa Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi

11. Na hapana shaka Mwenyezi Mungu atawatambulisha walio amini, na atawatambulisha wanaafiki.¹¹

12. Na walio kufuru waliwaambia walio amini: Fuateni njia yetu, nasi tutayabeba makosa yenu. Wala wao hawatabeba katika makosa yao chochote kile. Hakika hao ni waongo.¹²

13. Na hapana shaka wataibeba mizigo yao na mizigo mingine pamoja na mizigo yao. Na kwa yakini wataulizwa Siku ya Kiyama juu ya waliyo kuwa wakiyazua.¹³

14. Na hakika tulimtuma Nuhu kwa watu wake, na akakaa nao miaka elfu kasoro miaka khamsini. Basi tufani liliwachukua, nao ni madhaalimu.¹⁴

15. Nasi tukamwokoia yeye na wenziwe wa katika safina, na tukaifanya kuwa ni Ishara kwa walimwengu wote.¹⁵

16. Na Ibrahim pale alipo waambia watu wake: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na mcheni Yeye. Hiyo ndiyo kheri yenu, ikiwa nyinyi mnajua.¹⁶

17. Hakika nyinyi mnaabudu masanamu badala ya Mwenyezi Mungu, na mnazua uzushi. Hakika hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu hawakumilikiini riziki yoyote. Takeni riziki kwa Mwenyezi Mungu, na mumuabudu Yeye, na mumshukuru Yeye. Kwake Yeye ndio mtarudishwa.¹⁷

18. Na mkikadhibisha, basi kaumu kadhaa wa kadhaa za kabla yenu zilikwisha kadhibisha. Na si juu ya Mtume ila kufikisha Ujumbe waziwazi.¹⁸

19. Je! Wao hawaoni jinsi Mwenyezi Mungu anavyo anzisha uumbaji, na kisha

Mungu anayajua yaliomo vifuani mwa watu, ikiwa unaafiki au Imani.

11 Na hapana shaka Mwenyezi Mungu atawadhihirishia watu yale ambayo Yeye anayajua tangu hapo. Atawatenga mbali mbali baina ya Waumini na wanaafiki. Na kila mmoja atamlipa kwa alilo litenda.

12 Waongozi wa shirki walikuwa wakiwaambia wale walio ingia katika Uislamu kwa usafi wa niya: Kueni kama mliyvo kuwa katika dini yetu. Na fuateni tunayo fuata sisi. Na ikiwa kama huko kutakuwapo kufufuliwa na kuhisabiwa ambako nyinyi mnakuogopa, basi sisi tutakubebeen madhambi yenu. Hapana mtu atakayembebea mwenzie dhambi zake. Hakika hao makafiri ni waongo tu katika hiyo ahadi yao.

13 Basi makafiri wataibeba wenyewe mizigo yao mizito, na juu ya hiyo watabeba mfano wa mizigo ya wale walio wapoteza na wakawazua wasiifuate Haki. Na hapana shaka yoyote watahisabiwa Siku ya Kiyama kwa walio kuwa wakiyazua ya uwongo duniani, na watapewa adhabu kwa hayo.

14 Na Mwenyezi Mungu alimtuma Nuhu ende kwa watu wake awaite wafuate Tawhidi, Imani ya Mwenyezi Mungu Mmoja. Akakaa nao miaka mia tisa na khamsini akiwalingania. Nao hawakumuitikia. Mwenyezi Mungu akawazamisha kwa kuwapelekea tufani (kimbunga), nao ni wenye kujidhulumu nafsi zao kwa ukafiri.

15 Mwenyezi Mungu akamtimilizia Nuhu ahadi yake, na akamwokoia yeye na Waumini walio panda naye jahazi. Na akakifanya kisa chao ni funzo kwa walio kuja baadae.

16 Na kumbuka, ewe Mtume, kisa cha Ibrahim, pale alipo wataka watu wake wamuamini Mwenyezi Mungu Mmoja na wamt'ii Yeye, na akawanabihisha kwamba kuamini ni bora kwao kuliko kukanusha, ikiwa wao wana ujuzi na akili.

17 Akawaambia: Nyinyi hamuabudu badala ya Mwenyezi Mungu ila vinyago na masanamu mnayo yaunda kwa mikono yenu. Na mnazua uwongo na mnayaita kuwa miungu. Na haya masanamu mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu hayakufaini wala hayakudhuruni, wala hayawezi kukupatieni riziki. Basi tafuteni riziki kwa Mwenyezi Mungu peke yake, na muabuduni Yeye tu, na mshukuru Yeye tu kwa neema zake. Kwani kwake Yeye ndio marejeo yenu nyote, naye atakulipeni kwa mujibu wa vitendo vyenu.

18 Na mkishikilia kunikadhibisha mimi basi hamtanidhuru kitu. Kwani bila ya shaka nimekwisha kwambieni kwamba Mitume wa kabla yangu walikanushwa na kaumu zao, na hawakuwadhuru kitu, bali walijidhuru wenyewe nafsi zao, pale Mwenyezi Mungu alipo waangamiza kwa sababu ya kukadhibisha kwao. Basi Mjumbe hana jukumu lolote ila kufikisha Ujumbe wake kwa kaumu yake kwa uwazi.

akarudisha tena. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.¹⁹

20. Sema: Tembeeni katika ardhi na tazameni jinsi alivyo anzisha uumbaji; kisha Mwenyezi Mungu ndiye anaye umba umbo la baadaye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.²⁰

21. Humuadhibu amtakaye, na humrehemu amtakaye. Na kwake Yeye mtapelekwa.²¹

22. Na nyinyi si wenye kushinda katika ardhi wala katika mbingu. Wala nyinyi hamna mlinzi wala msaidizi isipo kuwa Mwenyezi Mungu.²²

23. Na walio zikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu na kukutana naye, hao ndio wenye kukata tamaa na rehema yangu, na hao ndio wenye kupata adhabu chungu.²³

24. Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila ni kusema: Muuweni au mchomeni moto! Mwenyezi Mungu akamwoko na moto. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanao amini.²⁴

25. Na alisema: Hakika nyinyi mmeyashika masanamu badala ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yaliyo baina yenu katika uhai wa duniani. Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi, na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi. Na makaazi yenu ni Motoni. Wala hamtapata wa kukunusuruni.²⁵

26. Lut'i akamuamini, na akasema: Mimi nahamia kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.²⁶

19 Hakika wamekwisha ona na wamejua kwamba hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliye anzisha uumbaji, na akisha akaurudisha tena. Basi vipi ikawa wanakanusha kufufuliwa Siku ya Akhera kwa ajili ya hisabu na malipo? Hakika kurejesha tena kwa Mwenyezi Mungu ni jambo jepesi zaidi.

20 Ewe Mtume! Waambie hawa wanao kanusha: Tembeeni katika ardhi, na zingatieni vilivyo vitu mbali mbali alivyo viumba Mwenyezi Mungu. Na angalieni mabaki ya waliyo kuwa kabla yenu, baada ya kwisha kufa kwao na majumba yao waliyo yaacha. Na jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu kwa kudra yake atayarejesha yote hayo mwishoe kwa kufufua, nako ndiko huko kuumba umbo la baadaye. Hali kadhaalika shani yenu. Hakika Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni Mwenye kutimia uwezo wake juu ya kila kitu. (*Tazama Maelezo 29:20*)

21 Mwenyezi Mungu atawaadhibu awatakaye baada ya uumbaji mwingine, na hao ndio wale wenye kukanusha hayo. Na atawarehemu awatakaye, nao ndio Waumini wenye kuyakubali hayo. Na kwake Yeye peke yake ndio marejeo ya viumbe vyote kwa ajili ya hisabu na malipo.

22 Enyi mnao kadhibisha! Nyinyi hamtaweza kuishinda kudra ya Mwenyezi Mungu; sawa sawa mkiwa katika ardhi au katika mbingu. Bali hiyo kudra yake imekuzungukeni nyinyi. Wala nyinyi hamna mlinzi wa kukulindeni na Mwenyezi Mungu, wala msaidizi wa kukuzuilieni adhabu yake.

23 Na wale wanao zikataa dalili za Mwenyezi Mungu zinazo thibitisha upweke wake, na wakawakadhibisha Mitume wake na Vitabu vyake, na wakakanusha kufufuliwa na kuhisabiwa - watu hao hawana tamaa ya kupata rehema ya Mwenyezi Mungu. Na watu hawa watapata adhabu kali yenye kutia chungu.

24 Na pale Ibrahim alipo waamrisha watu wake wamuabudu Mwenyezi Mungu na waache ile ibada ya masanamu waliyo kuwa nayo, hawakuwa na jawabu yoyote ya kumjibu ila kukakamia katika ukafiri, na kuambizana wenyewe kwa wenyewe: Muuweni, au mchomeni moto! Basi wakamtupa motoni. Lakini Mwenyezi Mungu akaufanya moto uwe baridi na wenye salama kwake. Na akamwoko nao. Hakika kwa kubwatika vitimbi vyao na kuokoka kwake zipo dalili zilizo wazi kwa watu wanao isadiki Tawhid (upweke) wa Mwenyezi Mungu na kudra yake.

25 Ibrahim akawaambia watu wake: Kwa nini mnaabudu miungu ya uwongo, na wala hamkatazani, kwa sababu ya mapenzi ya madhambi mliyo yakhiari katika maisha yenu ya dunia? Kisha hali itabadilika Siku ya Kiyama. Huko waongozi watawakataa wafuasi wao. Na wafwasi watawalaani waongozi wao. Na marejeo ya wote ni Motoni. Wala hamtakuwa na msaidizi wa kukuzuilieni msiingie humo.

26 Na alikuwa katika wa mwanzo wa kuitikia wito wa Ibrahim, ni Lut'i. Akasadiki, na kabla yake alikuwa kesho kuwa mwenye kushika Tawhid. Na Ibrahim akasema kwa kut'i amri ya Mwenyezi Mungu: Mimi ninahama kwendea upande aliyo niamrisha Mola wangu Mlezi nihamie, na nikakae na huko niwaitie watu wamfuute Mwenyezi Mungu. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu wa kuweza kunilinda na maadui zangu,

27. Na tulimtukia (Ibrahim) Is-haq na Yaa'qub. Na tukajaalia katika dhuriya zake Unabii na Kitabu, na tukampa ujira wake katika dunia; naye hakika katika Akhera bila ya shaka ni katika watu wema.²⁷

28. Na pale Lut'i alipo waambia watu wake: Hakika nyinyi mnafanya uchafu, ambao hapana mmoja katika walimwengu aliye kutangulieni kwa hayo.²⁸

29. Je! Nyinyi mnawaingilia wanaume, na mnaikata njia? Na katika mikutano yenu mnafanya maovu? Basi haikuwa jawabu ya watu wake isipo kuwa kusema: Tuletee hiyo adhabu ya Mwenyezi Mungu ikiwa wewe ni katika wasemao kweli.²⁹

30. Akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ninusuru na watu mafisadi hawa!³⁰

31. Na wajumbe wetu walipo mjia Ibrahim na bishara, walisema: Hakika sisi hapana shaka tutawahiliki watu wa mji huu, kwani watu wake hakika wamekuwa madhaalimu.³¹

32. Akasema: Hakika humo yumo Lut'i. Wao wakasema: Sisi tunajua zaidi nani yumo humo. Hapana shaka tutamwokoia yeye na ahali zake, isipo kuwa mkewe aliye miongoni mwa watao kaa nyuma.³²

33. Na wajumbe wetu walipo mfikia Lut'i, alihuzunika kwa ajili yao, na moyo uliona dhiki kwa ajili yao. Wakasema: Usiogope, wala usihuzunike. Hakika sisi tutakuokoa wewe na ahali zako, ila mkeo aliye miongoni mwa watao kaa nyuma.³³

34. Kwa yakini sisi tutawateremshia watu wa mji huu adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya uchafu wanao ufanya.³⁴

35. Na tumeacha katika mji huo Ishara ilio wazi kwa watu wanao tumia akili zao.³⁵

Mwenye hikima ambaye haniamrishi ila lilio la kheri.

27 Na Mwenyezi Mungu akamtukia Ibrahim kwa kumpa mwana, naye ni Is-haq, na kumpa mjukuu, naye ni Yaa'qub. Na akamfanyia ukarimu kwa kumjaalia Unabii katika dhuriya zake, na kuwateremshia Vitabu vya mbinguni, na kwa kumlipa bora ya malipo katika dunia, naye huko Akhera kuwa ni miongoni mwa bora ya watu wema.

28 Na ewe Mtu! Kumbuka pale tulipo mtuma Lut'i kwa kaumu yake, akawataka waishike Tawhidi ya Mwenyezi Mungu na ut'iifu wake. Na akawakataza kitendo kichafu walicho kuwa wakikitenda, ambacho hajapata kukitenda yeyote katika viumbe vya Mwenyezi Mungu.

29 Hakika hayo myatendayo ni maovu na yanahilikisha. Kwani nyinyi mnawafanya mambo machafu wanaume, na mnaikata njia ya uzazi; na khatima ya hayo ni kutoweka kabisa. Na katika mikutano yenu mnatenda maovu bila ya kumkhofu Mwenyezi Mungu wala kuoneana haya baina yenu. Wala watu wake hawakumsikia, wala hawakuwa na jawabu ya kumpa ila kumfanyia maskhara tu. Na wakamtaka alete upesi hiyo adhabu ya Mwenyezi Mungu aliyo watishia kwayo, ikiwa yeye ni mkweli kwa hayo ayasemayo.

30 Basi Lut'i akamtaka msaada Mwenyezi Mungu kupambana nao, na akamwomba amnusuru juu ya watu wake wenye kufanya fisadi katika nchi.

31 Na walipo kuja Malaika wa Mwenyezi Mungu kwa Ibrahim, a.s. kwa kumbashiria, walisema kwamba wameamrisha kuwaangamiza watu wa mji huo kwa sababu ya kufisidi kwao na kujidhulumu kwao wenyewe kwa ushirikina na kutenda uchafu.

32 Ibrahim a.s. akawaambia Malaika: Hakika katika huo mji yumo Lut'i. Basi vipi mtawaangamiza hao naye yumo kati yao. Malaika wakamjibu kwamba wao wanajua nani waliomo humo, na kwamba wao kwa hakika watamwokoia Lut'i na ahali zake wasipate adhabu, isipo kuwa mkewe. Yeye huyo atakuwa miongoni mwa watao angamizwa kwa sababu ya ukafiri wake na uovu wake.

33 Walipo ondoka wale Malaika walio tumwa kumuendea Lut'i naye akawaona, alihuzunika kwa kuwakhofia uadui wa watu wake, na akaemewa asiwe na hila ya kuweza kuwalindia. Wao, basi, wakampoza na wakamwambia: Kabisa usiukhofu uadui wa kaumu yako juu yetu, wala usihuzunike kwa ajili yetu. Kwani sisi hakika tumekuja kuwaangamiza watu wa mji huu, na tutakuokoa wewe na ahali zako. Lakini mkeo atakuwa pamoja na wenye kuangamia.

34 Malaika wakasema: Hakika sisi tumetumwa kutimiliza amri ya Mwenyezi Mungu kwa kuwateremshia watu wa mji huu adhabu itokayo mbinguni kwa sababu ya uchafu wao na ukafiri wao.

35 Na Mwenyezi Mungu akauteketeza mji huu, na akaacha humo mabaki yaliyo wazi, ili yawe ni dalili ya

- 36.** Na kwa Madyana tulimtuma ndugu yao Shuaibu, naye akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu na iogopeni Siku ya Akhera, wala msende katika ardhi mkifisidi.³⁶
- 37.** Lakini walimkanusha basi ukawatwaa mtikiso wa ardhi, wakapambazukiwa ndani ya nyumba zao nao wamefudikia.³⁷
- 38.** Na pia kina A'di na Thamud. Nanyi yamekwisha kubainikieni kutokana na maskani zao. Na Shet'ani aliwapambia vitendo vyao, na akawazuilia Njia, na hali walikuwa wenye kuona.³⁸
- 39.** Na pia Qaruni na Firauni na Hamana! Na Musa aliwajia kwa Ishara waziwazi, lakini walijivuna katika nchi, wala hawakuweza kushinda.³⁹
- 40.** Basi kila mmoja tulimtesa kwa mujibu wa makosa yake. Kati yao wapo tulio wapelekea kimbunga cha changarawe; na kati yao wapo walio nyakuliwa na ukelele; na kati yao wapo ambao tulio wadidimiza katika ardhi; na kati yao wapo tulio wazamisha. Wala Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuwadhulumu, lakini walikuwa wenyewe wakijidhulumu nafsi zao.⁴⁰
- 41.** Mfano wa walio wafanya walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, ni mfano wa buibui alivyo jitandia nyumba. Na hakika nyumba dhaifu mno kuliko zote ni jumba la buibui, laiti kuwa wanajua.⁴¹
- 42.** Kwa hakika Mwenyezi Mungu anajua kila kitu wanacho kiomba badala yake Yeye. Na Yeye ndiye Mtukufu Mwenye nguvu Mwenye hikima.⁴²

kuonyesha aliyowafanyia Mwenyezi Mungu, na funzo kwa mwenye kuzingatia.

36 Na Mwenyezi Mungu aliwapelekea watu wa Madyana Mtume kutokana nao wenyewe, naye ni Shuaibu. Akawaita waishike Tawhidi ya Mwenyezi Mungu, na wamuabudu Yeye tu, na waiogope Siku ya Mwisho, na watende vitendo ambavyo kwavyo watumai kupata malipo mema kwa Mwenyezi Mungu, na akawakataza kukimbilia kutenda ufisadi katika nchi.

37 Wakamkanusha na wakamuasi. Basi Mwenyezi Mungu akawaangamiza kwa tetemeko kubwa mno lilio wavunjia majumba yao. Wakawa humo wameanguka maiti.

38 Na ewe Mtume! Watajia hawa walio danganyikiwa kwa mali zao na madaraka yao vifo vya A'di na Thamudi pale tulipo waangamiza. Na yapo yamebakia mabaki ya majumba yao yenye kuonyesha utajiri wao. Na sababu ya kuangamizwa huko ni kwa kuwa Shetani aliwazaini, aliwapambia vitendo vyao viovu, nao wakamfuata. Basi akawaachisha Njia ya Haki ambayo walikuwa wakijua kwa kufunzwa na Mitume.

39 Na ewe Mtume! Watajia hawa walio ghurika kwa mali yao na madaraka yao, kifo cha Qaruni na Firauni na Hamana na yaliyo wapata katika ada ya Mwenyezi Mungu kuwahiliki wakanushao. Na Mwenyezi Mungu aliwatumia Musa naye akawa na miujiza iliyo wazi ya kuthibitisha ukweli wake. Lakini wao walimkadhibisha, na wakakataa kumuitikia kwa kiburi chao tu. Na wala wao hawakuweza kuishinda kudra ya Mwenyezi Mungu kwa kuikimbia adhabu yake.

40 Kila kaumu katika kaumu zote zilizo wakadhibisha Mitume wao Mwenyezi Mungu ameziangamiza kwa sababu ya kufuru zao walizo zifanya na maasi yao. Baadhi ya kaumu hizo Mwenyezi Mungu alizihiliki kwa upepo wa kimbunga ulio wapopoa kwa mawe. Na baadhi yao waliangamia kwa ukelele wenye kuvuma wenye kuhiliki. Na baadhi yao Mwenyezi Mungu aliwadidimiza katika ardhi. Na baadhi yao aliwazamisha majini. Wala adhabu hizi hazikuwa ni kudhulumuwa na Mwenyezi Mungu, bali sababu yake ni kwa kufuru yao wenyewe na kutenda maasi kwao.

41 Shani ya hao waongo wenye kumfanya urafiki asiye kuwa Mwenyezi Mungu na kumtegemea asiye faa kutegemewa, ni kama shani ya buibui mwenye kuifanya nyumba ya kumlinda, na hali nyumba yake ndiyo nyumba isiyo faa kabisa kutumika kwa ulinzi. Na lau kuwa hawa waongo ni watu wa ujuzi na utambuzi wasinge fanya hayo. (*Tazama Maelezo 29:41*)

42 Hakika Mwenyezi Mungu, *Subhanahu*, anajua vyema upotovu wa kuwaabudu hiyo miungu ya uwongo. Na Yeye *Subhanahu* ndiye Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye hikima katika kuendesha na kuweka sharia.

- 43.** Na hiyo ni mifano tunawapigia watu, na hawaifahamu ila wenye ilimu.⁴³
- 44.** Mwenyezi Mungu ameumba mbingu na ardhi kwa Haki. Kwa hakika katika hayo ipo Ishara kwa Waumini.⁴⁴
- 45.** SOMA uliyo funuliwa katika Kitabu, na ushike Sala. Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yatenda.⁴⁵
- 46.** Wala msjadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa, isipo kuwa wale walio dhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeyaamini yaliyo teremshwa kwetu na yaliyo teremshwa kwenu. Na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja. Na sisi ni wenye kusilimu kwake.⁴⁶
- 47.** Na namna hivi tumekuteremshia Kitabu (cha Qur'ani). Basi wale tulio wapa Kitabu (cha Biblia) wataiamini (Qur'ani), na miongoni mwa hawa (washirikina) wapo watacao iamini. Na hawazikatai Ishara zetu isipo kuwa makafiri.⁴⁷
- 48.** Na wewe hukuwa kabla yake unasoma kitabu chochote, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kulia. Ingeli kuwa hivyo wangelifanya shaka wavunjifu.⁴⁸
- 49.** Bali hii (Qur'ani) ni Ishara zilizo wazi katika vifua vya walio pewa ilimu. Na hawazikatai Ishara zetu isipo kuwa wenye kudhulumu.⁴⁹
- 50.** Na walisema: Mbona hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake Mlezi? Sema: Ishara ziko kwake Mwenyezi Mungu; ama mimi kwa hakika ni mwonyaji mwenye kubainisha tu.⁵⁰
- 51.** Je! Kwani hayakuwatosha ya kwamba tumekuteremshia Kitabu hiki wanacho

43 Na mazingatio haya na mifano hii, Mwenyezi Mungu anawatajia watu ili wawaidhike na wazingatie. Na hawazingatii haya ila wenye akili ambao wanapima.

44 Mbali na aliyoyataja Mwenyezi Mungu ya visa na mifano na ishara ipo Ishara moja iliyo wazi kabisa, nayo ni uumbaji wa mbingu na ardhi kwa uwezo na hikima, na kipimo kilicho kamilika, kwa maslahi ya watu. Na katika haya zipo dalili za kweli kwa wenye kuiamini Haki.

45 Ewe Nabii! Soma Kitabu cha Mwenyezi Mungu, wala usiwashughulikie. Na timiza Sala kwa inavyo stahiki. Kwani Sala pamoja na ikhlasi, kwa dhati yake humwachisha, mwenye kuishika, madhambi makubwa na kila maovu yanayo katazwa na Sharia. Na bila ya shaka, kumcha Mwenyezi Mungu, na kumhudhurisha kwa kumkumbuka katika Sala na kwengineko kuna athari kubwa zaidi na thawabu nyingi zaidi. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yatenda, yakiwa ya kheri au shari. Naye atakulipeni kwayo.

46 Wala msjadiliane na wanao kukhalifuni katika Mayahudi na Wakristo ila kwa njia yenye uwongofu kabisa, na laini kabisa, na inayo pelekea zaidi kukubalika. Isipo kuwa wale walio pita mpaka katika ubishi, basi hao hapana ubaya mkiwakabili kwa mkazo. Na waambieni mnao jadiliana nao: Sisi tumeiamini Qur'ani tulio teremshiwa sisi, na Taurati na Injili mlizo teremshiwa nyinyi. Na tunaye muabudu sisi, na mnaye muabudu nyinyi, ni mmoja. Na sisi tunamnyenyekea Yeye peke yake.

47 Na kama tulivyo wateremshia vitabu Mitume wa kabla yako, tumekuteremshia wewe hii Qur'ani. Basi wale tulio wapa Kitabu (Biblia) kabla ya Qur'ani, na wakaizingatia na wakaifuata, wanaiamini hii Qur'ani. Na miongoni mwa hawa Waarabu (washirikina) wapo wanao iamini. Na hapana wanao zikataa Ishara zetu - baada ya kudhihiri kwake na kuondoka kila shaka juu yake - ila walio shikilia ukafiri.

48 Wala wewe hukuwa ukisoma kitabu chochote kabla ya Qur'ani. Wala hukuwa ukiandika kwa mkono wako wa kulia. Na lau kuwa wewe ni katika ya wanao soma na kuandika wangetilia shaka watu wapotovu kuwa hiyo Qur'ani haitoki kwa Mwenyezi Mungu.

49 Kitabu hichi si cha kutiliwa shaka, bali hizi ni Ishara zilizo wazi zilizo hifadhiwa katika vifua vya watu ambao Mwenyezi Mungu amewapa ilimu. Na hazikatai Ishara zetu, baada ya kuzijua, ila wenye kuidhulumu Haki na wakazidhulumu nafsi zao.

50 Na makafiri katika majadiliano yao na ukaidi wao walisema: Mbona hakuteremshiwa miujiza ya kuiona kwa macho kama iliyo wateremkia Mitume wa kabla yake? Waambie: Miujiza yote iko kwa Mwenyezi Mungu. Huitemsha anapo taka. Ama mimi nimetumwa kuonya kwa uwazi, sio kuleta hayo mtakayo.

somewa? Hakika katika hayo zipo rehema na mawaidha kwa watu wanao amini.⁵¹

52. Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa ni Shahidi baina yangu na nyinyi. Anayajua yaliomo katika mbingu na ardhi. Na wale wanao amini upotovu na wakamkataa Mwenyezi Mungu, hao ndio walio khasiri.⁵²

53. Na wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka. Na lau kuwa hapana wakati maalumu ulio wekwa, basi adhabu ingeli wajia, na ingeli watokea kwa ghafla, na hali wao hawana khabari.⁵³

54. Wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka, na hali Jahannamu kwa hakika imewazunguka makafiri!⁵⁴

55. Siku itapo wafunika adhabu hiyo kutoka juu yao na chini ya miguu yao, na atasema: Onjeni hayo mliyo kuwa mkiyatenda!⁵⁵

56. Enyi waja wangu mlio amini! Kwa hakika ardhi yangu ina wasaa. Basi niabuduni Mimi peke yangu.⁵⁶

57. Kila nafsi itaonja mauti. Kisha mtarudishwa kwetu.⁵⁷

58. Na ambao wameamini na wakatenda mema, bila ya shaka tutawaweka katika maghorofa ya Peponi yenye kupitiwa chini yake mito, wakidumu humo. Ni mwema ulioje huo ujira wa watendao,⁵⁸

59. Ambao walisubiri, na wakamtegemea Mola wao Mlezi.⁵⁹

60. Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Mwenyezi Mungu anawaruzuku hao na nyinyi pia. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua.⁶⁰

51 Wanataka Ishara hizo, nao haiwatoshi wao kuwa Sisi tumekuteremshia hichi Kitabu wanacho somewa? Na huu ndio Muujiza wa kudumu milele na zingapita zama. Hakika kwa kuteremka Kitabu hichi juu yako bila ya shaka ni rehema kwao na kwa vizazi vyote vijavyo baada yao, na ni kumbusho la daima dawamu lenye manufaa kwa watu ambao shani yao ni kuamini wanapo onyeshwa wazi Njia ya Uwongofu.

52 Sema: Yanitosha mimi na yakutosheni nyinyi ya kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Shahidi kuwa mimi nimefikisha niliyo tumwa kwenu. Na hayo ndiyo chanzo cha mambo yangu na mambo yenu. Wala hakifichiki kwake chochote cha mbinguni na duniani. Na walio muabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na wakamkataa Mwenyezi Mungu na wasimkhusishe Yeye tu kwa ibada, hao ndio walio nunua ukafiri kwa Imani, na wakasibiwa na khasara iliyo wazi.

53 Na makafiri wanakufanyia ushindani ya kuwa kama unaweza basi waletewe kwa haraka hiyo adhabu ulio waonya kuwa itawapata. Na lau kuwa wakati maalumu haukuwekwa kwa mujibu wa hikima yetu, tungeli waletewa kwa haraka hiyo adhabu wanayo ihimiza. Ninaapa itawatokea kwa ghafla, na hali wao hawana khabari.

54 Wanakutaka waletewe upesi adhabu, nayo itawajia tu, hapana hivi wala hivi. Na hakika, Jahannamu imewazunguka makafiri kwa yakini.

55 Siku itapo wafunika adhabu kutoka juu, licha ya kutoka chini, na Malaika aliye wakilishwa kuwaadhibu atapo sema: Onjeni jazaa ya hayo maovu mliyo kuwa mkiyatenda!

56 (Mwenyezi Mungu anasema:) Enyi waja wangu mlio niamini Mimi na Mtume wangu! Hakika ardhi yangu ni kunjufu kwa atakaye kukimbia kutoka katika nchi za shirki. Kimbieni mje kwangu mpatе kunisafia Mimi ibada.

57 Kila nafsi itaonja uchungu wa mauti bila ya shaka yoyote. Kisha mtarejea kwetu, na mtakuja lipwa kwa hayo mliyo yatanguliza, ikiwa ya kheri au ya shari.

58 Na walio muamini Mwenyezi Mungu na Vitabu vyake na Mitume wake, na wakatenda vitendo vyema, tunaapa kwamba bila ya shaka tutawaweka katika makaazi ya starehe kwenye maghorofa yapitayo mito chini yake. Neema zake haziwakatiki. Ni nzuri mno jazaa hii kuwa ni ujira wa wenye kutenda, wenye kusubiri kwa yanayo wapata kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wanapo acha nchi zao na watu wao na mali yao, nao wakimtegemea Mwenyezi Mungu peke yake katika hali zao zote.

59 Tazama tanbihi ya 58.

60 Na wanyama wengi wanao ishi nanyi katika ardhi ambao, kwa unyonge wao, hawawezi kubeba

61. Na ukiwauliza; Nani aliye umbwa mbingu na ardhi na akafanya jua na mwezi kuti'ii amri yake? Bila ya shaka, watasema: Mwenyezi Mungu. Wapi basi wanako geuzwa?⁶¹
62. Mwenyezi Mungu humkunjulia, na humdhikishia, riziki amtakaye katika waja wake. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.⁶²
63. Na ukiwauliza: Ni nani anaye teremsha maji kutoka mbinguni, na akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake? Bila ya shaka watasema: Ni Mwenyezi Mungu. Sema: Alhamdu Lillahi, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu. Bali wengi katika wao hawafahamu.⁶³
64. Na haya maisha ya dunia si chochote ila ni pumbao na mchezo. Na nyumba ya Akhera ndiyo maisha khasa; laiti wangeli kuwa wanajua!⁶⁴
65. Na wanapo panda katika marikebu, humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia ut'ifu. Lakini anapo wavua wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha.⁶⁵
66. Wapate kuyakanya tuliyo wapa, na wajistareheshe. Lakini watakuja jua!⁶⁶
67. Je! Hawaoni ya kwamba tumeifanya nchi takatifu ina amani, na hali watu wengine wananyakuliwa kote kwa majirani zao? Je! Wanaamini upotovu, na neema za Mwenyezi Mungu wanazikataa?⁶⁷
68. Na nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye mzulia uwongo Mwenyezi Mungu au anaye kanusha Haki inapo mjia? Je! Si katika Jahannamu ndio yatakuwa makaazi ya makafiri?⁶⁸

riziki yao na wakaihamisha kwa ajili ya kuila au kuiweka akiba. Ni Mwenyezi Mungu ndiye ambaye anawatengezea sababu za kuwaruzku na kuwaweka hai. Na Yeye anakutengenezeni nyinyi sababu za riziki zenu na maisha yenu. Na Yeye ni Mwenye kumiliki kila alichu kiumba kwa kusikia na kukijua.

61 Na ninaapa ukiwauliza washirikina: Nani aliye zumba mbingu na ardhi, na akalit'iiisha jua na mwezi, na akayafanya hayo yawanufaishe watu? Hapana shaka watasema: Kaviumba hivyo Mwenyezi Mungu. Wala hawamtaji mwengine. Basi inakuwaje wanaacha kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja Mtukufu, baada ya kukiri kwao huku?

62 Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye, na humdhikishia amtakaye, kwa mujibu wa inavyo wafikiana na ujuzi wake kwa ajili ya maslahi. Kwani hakika Mwenyezi Mungu amevizunguka vitu vyote kwa ujuzi wake.

63 Ninaapa, lau kuwa utawauliza: Nani anaye teremsha maji kutoka mbinguni, na akaihuisha ardhi kwa mimea baada ya kuwa na ukame? Hapana shaka watasema: Ni Mwenyezi Mungu. Sema: Alhamdu Lillahi, kuwa wanaikubali Haki. Lakini wengi wao hawafahamu kuwa wenyewe wanajitia katika migongano ya maneno.

64 Na haya maisha ya duniani si chochote ila ni starehe ya muda wenye ukomo. Wanapumbazika walio ghafilika kama wanavyo pumbazika watoto wadogo, na wanacheza kwa muda fulani na kisha wanatawanyika. Na hakika makaazi ya Akhera ndio makaazi ya maisha ya kweli, yaliyo kamilika, yenye kudumu. Na kweli hizi ni zenye kushibiti, wangeli zitambua hawa lau kuwa ni watu wa kutambua vilivyo.

65 Hao kwa walivyo sifika kwa ushirikina, wakipanda vyombo vya baharini, na wakapata kidogo katika vitisho vyake, humuelekea Mwenyezi Mungu kwa kumwomba kwa ikhlasi ili awaondolee madhara. Na akisha waokoa akawafikisha nchi kavu mara hukimbilia kurejea kwenye ushirikina.

66 Ili wapate kuzikanya neema tulizo wapa, na wapate kunafiika kwa yale yanayo ridhiana na pumbao lao katika maisha haya. Basi watakuja yajua matokeo ya ukafiri pale watapo iona adhabu iliyo chungu.

67. Makafiri wa Makka wameingia upofu, hawazioni neema za Mwenyezi Mungu alizo wamiminia, wala hawaoni kwamba hakika Sisi tumeufanya mji wao kuwa umehifadhika, haushambuliwi wala hauvamiwi, mtakatifu; watu wake hawatekwi nyara, wala ndani yake havitokei vita. Na hali kote jirani zao watu wananyakuliwa! Hawa wamepofuka hawazioni neema hizi, basi wanasadiki yasiyo na asli yoyote, na wanamkanusha Muhammad na yote aliyo yaleta!

68 Na hapana aliye dhulumu zaidi kuliko yule anaye msingizia Mwenyezi Mungu jambo ambalo hakulitolea sharia, au akaikadhibisha Dini ya Haki inapo mfikilia. Hakika katika Jahannam ndiko kwenye makaazi ya watu hawa madhaalimu, makafiri.

69. Na wanao fanya juhudi kwa ajili yetu, Sisi tutawaongoa kwenye njia zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na watu wema.⁶⁹

69 Na wale walio fanya ukomo wa juhudi zao, na wakastahamili mashaka kwa sababu ya kuinusuru Dini yetu, hapana shaka tutawazidishia kuwaongoa kuendea kheri na Haki. Na hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka yu pamoja na wale wanao fanya vizuri vitendo vyao; atawasaidia na atawanusuru. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi kuliko wote.

Sura 30 - Ar-Rum

Utangulizi

SURA hii imeanza kutaja kushindwa kwa dola ya Rumi, na ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa Waumini kwamba atawapa ushindi kuwashinda Waajemi, na ikawataka watu wafikiri juu ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu, na watembe katika ardhi wapate kuujua mwisho wa makafiri walio iamirisha ardhi zaidi kuliko walivyo iamirisha wao Makureshi. Na Sura hii imeeleza hali ya watu Siku ya Kiyama, na ikasifu kutakasa kwa Waumini kumtakasa Mwenyezi Mungu, na wanavyo muabudu Yeye asubuhi mapema na jioni, na aduhuri na alasiri. Na ikanabihisha dalili za Upweke wake Mwenyezi Mungu kwa kupishana zamu usiku na mchana, na kukhitalifiana lugha, na mambo yanayo onekana ya ulimwengu katika mbingu na ardhi. Na ikapiga mifano ambayo inayo onyesha upotovu wa shirki, na ikawakumbusha watu vipi Mwenyezi Mungu alivyo waumba wao na akawaneemesha, na kuvitia nguvu viungo vya ukoo, na kushikamana kwa ujamaa, na ikashughulikia mambo ya sharia, ikaharimisha riba, na ikalazimisha Zaka, na ikahimiza kuwafanyia wema jamaa.

Kisha Mwenyezi Mungu *Subhanahu* akawaneemesha waja wake na akawataka washike Dini na ut'iifu, na akawataka waangalie katika ulimwengu yale maajabu yake yanayo onyesha ukomo wa nguvu na uweza. Na akabainisha mabadiliko ya binaadamu anavyo geuka mpaka akafikia umri wa ukongwe kabisa.

Na Aya za mwisho zimegusia Siku ya Kiyama na jinsi washirikina wanavyo ikanya. Na Sura ikakhitimishia kwa kumnasih Mtume s.a.w. athibiti juu ya Haki, na avumilie kwa yanayo mfika, kwani ahadi ya Mwenyezi Mungu inakuja tu bila ya muhali wowote.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Mim (A.L.M.)¹

2. Warumi wameshindwa,²

3. Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda³

4. Katika miaka michache. Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake. Na siku hiyo Waumini watafurahi.⁴

5. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye

1 Sura hii imeanzia kwa Aya hii ili kufahamisha kwamba Qur'ani imetungwa kwa hizi hizi harufi wanazo zitamka Waarabu kwa wepesi na kwa uwazi. Lakini wanao kanya wameshindwa kuleta mfano wake. Nazo vile vile zinawazindua watu wasikilize na wanyamaze, na ziwapelekee kuusadiki Utume wa Muhammad s.a.w.

2 Waajemi waliwashinda Warumi katika nchi ya karibu na Arabuni, nayo ni mipakani mwa Shamu. Nao Warumi baada ya kushindwa kwao watakuja washinda Waajemi.

3 Tazama tanbihi ya 2.

4 kabla ya kupita miaka tisa. Na washirikina walifurahi kwa kushinda Waajemi, na wakawaambia Waislamu: Tutakushideni kama Uajemi ilivyo ushinda Urumi ambayo ni katika Watu wa Kitabu. Lakini Mwenyezi Mungu alitimiza ahadi yake, Warumi wakawashinda Waajemi kwa muda ule ule alio utaja. Ikawa ile ni Ishara ya ukweli wa Muhammad s.a.w. katika wito wake, na ukweli wa aliyo yaleta. Ni ya Mwenyezi Mungu amri na hukumu kabla ya kila kitu na baada ya kila kitu. Na siku ya Warumi kuwashinda Waajemi watafurahi Waumini kwa ajili ya ushindi wa Mwenyezi Mungu anao mpa amtakaye. Na Yeye ndiye Mwenye kuwashinda maadui zake, Mwenye kuwarehemu vipenzi vyake. (Tazama Maelezo 30:4)

nguvu Mwenye kurehemu.⁵

6. Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake. Lakini watu wengi hawajui.⁶

7. Wanajua hali ya dhaahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.⁷

8. Je! Hawajifikirii nafsi zao? Mwenyezi Mungu hakuumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yake ila kwa Haki na kwa muda maalumu. Na hakika watu wengi bila ya shaka ni wenye kukataa kuwa watakutana na Mola wao Mlezi.⁸

9. Je! Hawatembei katika ardhi wakaona ulivyo kuwa mwisho wa walio kuwa kabla yao? Nao walikuwa na nguvu zaidi kuliko wao, na wakaitimbua ardhi na wakaistawisha zaidi kuliko walivyo istawisha wao. Na Mitume wao wakawajia na dalili zilizo wazi. Basi hakuwa Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwadhulumu, lakini walikuwa wakijidhulumu nafsi zao.⁹

10. Kisha ulikuwa mwisho wa walio fanya ubaya ni kuzikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakawa wanazifanyia maskhara.¹⁰

11. Mwenyezi Mungu huanzisha uumbaji, tena akaurudisha mara ya pili, na kisha mtarejeshwa kwake.¹¹

12. Na itapo simama Saa wakosefu watakata tamaa.¹²

13. Wala hawatakuwa na waombezi miongoni mwa walio kuwa wakiwashirikisha na Mungu; na wao wenyewe watawakataa hao washirikishwa wao.¹³

14. Na siku itapo simama Saa, siku hiyo watagawanyika.¹⁴

15. Ama walio amini na wakatenda mema watafurahishwa katika Bustani.¹⁵

5 Tazama tanbihi ya 4.

6 Mwenyezi Mungu ameagana na Waumini kwa agano la kweli. Na Mwenyezi Mungu havunji agano lake. Lakini makafiri, wanao kataa, si ada yao kujua mambo hakika yalivyo.

7 Wanajua mambo na njia za kuamirisha na kustarehe na mapambo yake, na hali wao wamepita mpaka katika ujinga na kughafilika kujitengenezea Akhera yao..

8 Yamefutwa macho yao na nyoyo zao, na hivyo hawajifikirii mambo yaliyo khusiana na roho zao wakaujua mwisho wao. Mwenyezi Mungu hakuziumba mbingu na ardhi na nyota na vinginevyo viliomo baina yao ila kwa kweli kweli, si mchezo, na kwa wakati ulio wekewa kiwango chake maalumu kitakacho kwisha. Na hakika wengi wa watu wanakataa kuwa watakuja kukutana na Mwenyezi Mungu, na kwamba itakuwapo Saa ya Kiyama.

9 Wao wameshikilia kukaa katika nchi zao tu, wala hawendi kote kote duniani wapate kushuhudia ulikuwaje mwisho wa walio kufuru wa kabla yao. Hao walikuwa na nguvu zaidi kuliko hawa makafiri wa sasa, na wakaugeza uso wa ardhi wapate kutoa humo viliomo ndani yake, kama maji, na maadeni, na makulima. Na wakaiaamirisha ardhi zaidi kuliko walivyo amirisha hawa. Na Mitume wa Mwenyezi Mungu wakawajia na miujiza iliyo wazi, na wao wakaikataa. Mwenyezi Mungu akawatia mkononi, kwani Yeye hawalipi bila ya makosa, wala hawashiki kabla ya kuwakumbusha na kuwapa muhula. Lakini watu hawakuwa wanadhulumu ila nafsi zao tu.

10 Tena mwisho wa hao watu walio tenda hadi ya uovu ni kuzikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakawa wanazidharau khasa.

11 Mwenyezi Mungu, aliye takasika na kutukuka, huanzisha uumbaji wa binaadamu tangu mwanzo. Kisha hurejea tena kuwaumba baada ya kwisha kufa kwao. Tena hao wote wanarejea kwake Yeye peke yake kwa ajili ya hisabu na malipo.

12 Na kikifika Kiyama makafiri watakata tamaa ya kuweza kujitetea nafsi zao.

13 Na wala hawapatikani waombezi kutokana na hao walio waabudu badala ya Mwenyezi Mungu na kwa sababu yao wakawa ni makafiri duniani.

14 Na itapo simama Saa, yaani Siku ya Kiyama, kila kikundi kitaandea kwenye ajali yake ya milele.

15 Ama walio amini, na wakaambatisha Imani yao na vitendo vyema, basi hao watakuwa katika Bustani yenye miti na mauwa, watafurahi na wataneemeka.

16. Na ama walio kufuru na wakazikanusha Ishara zetu na mkutano wa Akhera, hao basi watahudhurishwa katika adhabu.¹⁶
17. Basi *Subhanallah!* Mtakaseni Mwenyezi Mungu jioni na asubuhi,¹⁷
18. Na sifa zote njema ni zake katika mbingu na ardhi, na alasiri na adhuhuri.¹⁸
19. Hukitoa kilicho hai kutokana na kilicho kufa, na hukitoa kilicho kufa kutokana na kilicho hai. Na huihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Na kama hivyo ndivyo mtavyo fufuliwa.¹⁹
20. Na katika Ishara zake ni kuwa kakuumbeni kwa udongo. Kisha mmekuwa watu mlio tawanyika kote kote.²⁰
21. Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri.²¹
22. Na katika Ishara zake ni kuumba mbingu na ardhi, na kutafautiana ndimi zenu na rangi zenu. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa wajuzi.²²
23. Na katika Ishara zake ni kulala kwenu usiku na mchana, na kutafuta kwenu fadhila zake. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao sikia.²³
24. Na katika Ishara zake hukuonyesheni umeme kwa kukutieni khofu na tamaa. Na hukuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanao zingatia.²⁴
25. Na katika Ishara zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa amri yake. Kisha atakapo kuiteni mwito mmoja tu, hapo mtatoka kwenye ardhi.²⁵

16 Ama wale walio kufuru, na wakazikataa Ishara zetu na mkutano wa kufufuliwa na kuhisabiwa, basi hao watakuwa wanaishi katika adhabu, wala hawatoki humo.

17 Basi mtakaseni Mwenyezi Mungu na kila ambacho hakimuelekei kwa utukufu wake na ukamilifu wake. Na muabuduni Yeye mnapo ingia jioni na mnapo ingia asubuhi.

18 Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye kustahiki kuhimidiwa na kusifiwa na kushukuriwa na walioko katika mbingu na katika ardhi. Basi mhimidini na mumuabudu wakati wa alasiri na mnapo ingia adhuhuri.

19 Yeye hutoa kiumbe kihai kutokana na kitu kisicho kuwa na uhai. Na hukitoa kitu kisicho kuwa na uhai kutokana na kitu chenye uhai. Na huihuisha ardhi kwa mimea baada ya kuwa ni kavu tupu. Na mfano wa anavyo fanya hivi basi ndivyo hivyo Mwenyezi Mungu atakutoeni makaburini mwenu.

20 Na katika dalili za kuonyesha ukamilifu wa uweza wake ni kuwa ameumba asili yenu kutokana na udongo usio kuwa na uhai. Kisha nyinyi mmekuwa watu mlio tawanyika katika ardhi kwa ajili ya kutafuta kitacho kuleteeni kubaki kwenu

21 Na katika dalili za rehema yake ni kuwa kakuumbieni, enyi wanaume, wake wa jinsi yenu mkae nao kwa uzuri na kituo. Na amekujaalieni baina yenu na wao mapenzi na kuoneana huruma. Hakika katika haya bila ya shaka zipo dalili kwa watu wanao ufikiria uumbaji wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

22 Na katika dalili za kuonyesha uweza wake na hikima yake ni uumbaji wa mbingu na ardhi kwa mpango huu wa namna peke yake wenye kupendeza, na kukhitalifiana ndimi zenu katika lugha mbali mbali na lafdhi mbali mbali, na kutafautiana rangi zenu katika weusi na weupe na nyenginezo. Hakika katika haya bila ya shaka zipo dalili zinazo wanufaisha watu wenye ujuzi na kufahamu.

23 Na katika Ishara zake zenye kuonyesha ukamilifu wa uweza wake ni kuwa amekupeni sababu za mapumziko kwa kulala kwenu. na akakusahilishieni kutafuta riziki usiku na mchana kutokana na fadhila zake kunjufu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo dalili kwa watu wanao nafika kwa wanayo yasikia.

24 Na katika Ishara zake ni kuwa anakuonyesheni umeme katika mawingu, muone khofu kwa radi na tamaa ya kupata mvua ya kuteremka kutoka mbinguni ili ardhi ihuikie baada ya kuyabisika. Hakika katika hayo bila ya shaka zipo dalili kwa watu wanao zingatia mambo wakayafahamu kama ifaavyo.

25 Na katika dalili za ukamilifu wa uweza wake, na hikima yake, na ukunjufu wa rehema yake, ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa amri ya Mwenyezi Mungu, kama muonavyo, kwa mujibu wa hukumu za ufundi na ustadi wa kupanga. Kisha akikuiteni kwa ajili ya kukufufueni mtatoka makaburini mbio

26. Na vyake Yeye vilivyo mbinguni na katika ardhi. Vyote vinamt'ii Yeye.²⁶
27. Na Yeye ndiye anaye anzisha uumbaji, kisha ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi kwake. Naye ndiye mwenye mfano bora katika mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.²⁷
28. Amekupigieni mfano kutokana na nafsi zenu. Je! Katika hao iliyo wamiliki mikono yenu ya kulia mnao washirika katika hivyo tulivyo kuruzukuni, mkawa nyinyi katika hivyo ni sawasawa, mnawaogopa kama mnavyo ogopana wenyewe kwa wenyewe? Namna hivi tunazipambanua Aya zetu kwa watu wenye akili.²⁸
29. Bali walio dhulumu wamefuata mapendo ya nafsi zao pasina kujua. Basi nani atamwongoa ambaye Mwenyezi Mungu amemuacha apotee? Wala hao hawatakuwa na wa kuwanusuru.²⁹
30. Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.³⁰
31. Muwe wenye kutubia kwake, na mcheni Yeye, na shikeni Sala, na wala msiwe katika washirikina.³¹
32. Katika wale ambao kwamba wameigawanya dini yao, na wakawa makundi makundi, kila kikundi kinafurahia kilicho nacho.³²
33. Yakiwapata watu madhara humwomba Mola wao Mlezi nao wametubu kwake. Kisha akiwaonjesha rehema itokayo kwake, mara kikundi miongoni mwao

mbio kuitikia wito wake.

26 Na ni vyake Mwenyezi Mungu *Subhanahu* vyote viliomo katika mbingu na ardhi, kwa kuviumba, na kuvimiliki, na kunyenyekea. Vyote ni vyenye kumt'ii Mwenyezi Mungu.

27 Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* aliye umba viumbe vyote bila ya ruwaza, kisha atavirudisha tena baada ya mauti. Na kurudisha kwake ni jambo jepesi zaidi kuliko kuvizua mwanzo, kwa mujibu wa nadhari ya vipimo vyenu na itikadi yenu, kwamba kukirudisha kitu ni sahala kuliko kukizua. Na Mwenyezi Mungu ana sifa ya kutangulia ya shani ya namna ya pekee katika uweza ulio kamilika, na hikima iliyo timia, katika mbingu na ardhi. Na Yeye ni Mwenye kushinda katika ufalme wake, Mwenye hikima katika vitendo vyake na kukadiria kwake.

28 Mwenyezi Mungu amekupigieni mfano unao tokana na nafsi zenu - na Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwenye kutukuka amempigia mfano huo huyo aliye wafanya viumbe ni washirika wa Mwenyezi Mungu. Mfano wenyewe ni: Kwani nyinyi mnawafanya watumwa wenu washirika katika mali na vyenginevyo tulivyo kupeni? Basi, je! Nyinyi na wao ni sawasawa katika hayo, mnawaogopa hao watumwa wenu, na hamfanyi kitu kwa mnavyo miliki bila ya ruhusa yao, kama wanavyo ogopana waungwana wao kwa wao? Ikiwa nyinyi hamyatii akilini haya wala hamyafanyi, basi imekuwaje hata mnavifanya baadhi ya alivyo vimiliki Mwenyezi Mungu kuwa ni washirika wake? Kwa ufafanuzi kama huu tunawabainishia Aya watu ambao wanazingatia mifano inayo pigwa

29 Bali walio kufuru wanafuata pumbao zao bila ya kujua matokeo ya kufuru zao. Basi hapana yeyote aliye achiliwa na Mwenyezi Mungu kupotoka, atakaye ongoka. Wala hapana ataye waombea, na akawalinda na adhabu.

30 Basi elekeza uso wako, na uelekee kwenye Dini mbali na upotovu wao. Na shikamana na maumbile ya Mwenyezi Mungu alio waumbia watu. Nayo ni kuwa wao ni wenye kuikubali Tawhidi, Imani ya Mwenyezi Mungu Mmoja, wala si wenye kuikataa. Na haitakikani kuigeuza khulka hii. Huko ndio kuumbwa juu ya Tawhidi, nayo ndiyo Dini Iliyo Nyooka sawasawa. Lakini washirikina hawaujui ukweli huo.

31 Kuweni wenye kurejea kwake kwa kutubu! Na tendeni alio kuamrishi, na acheni alio kukatazeni. Na hifadhini Sala, wala msiwe katika wenye kumuabudu mwenginewe pamoja na Mwenyezi Mungu.

32 Katika walio igawanya dini yao, wakawa makundi mbali mbali, kila kikundi kinawania upande wake, na kila fungu miongoni mwao linafurahia kwa waliyo nayo, wanajidhania kuwa wao tu ndio wako katika haki.

humshirikisha Mola wao Mlezi,³³

34. Kwa kuyakataa tuliyo wapa. Basi stareheni. Mtakuja jua!³⁴

35. Au tumewateremshia hoja ambayo kwayo ndio wanafanya ushirikina?³⁵

36. Na watu tunapo waonjesha rehema huifurahia, na ukiwasibu uovu kwa iliyo yatanguliza mikono yao wenyewe, mara wanakata tamaa.³⁶

37. Kwani hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye na humdhikisha amtakaye? Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanao amini.³⁷

38. Basi mpe jamaa haki yake, na masikini, na msafiri. Hayo ni kheri kwa watakao radhi ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye kufanikiwa.³⁸

39. Na mnacho kitoa kwa riba ili kiongezeke katika mali ya watu, basi hakiongezeki mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini mnacho kitoa kwa Zaka kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio watao zidishiwa.³⁹

40. Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni, kisha akakuruzukuni, kisha anakufisheni, na kisha anakufufueni. Je! Yupo yeyote katika hao mnao washirikisha na Mwenyezi Mungu afanyae lolote katika hayo? Yeye ametakasika, na ametukuka na hayo mnyo mshirikisha naye.⁴⁰

41. Ufisadi umedhihiri bara na baharini kwa iliyo yafanya mikono ya watu, ili Mwenyezi Mungu awaonyeshe baadhi ya waliyo yatenda. Huenda wakarejea kwa kutubu.⁴¹

42. Sema: Safirini duniani muangalie ulikuwaje mwisho wa walio tangulia. Wengi wao walikuwa washirikina.⁴²

33 Na watu yakiwapata madhara, ya ugonjwa au shida yoyote, humkimbilia Mwenyezi Mungu, na wakamwomba nao wamerejea kwake, wakitaka waondolewe hiyo shida. Kisha akiwaonjesha kuondokewa na hiyo shida, na akawapa sehemu ya fadhila yake, baadhi yao hukimbilia mbio kwendea kumshirikisha Mola wao Mlezi.

34 Upate kuwa mwisho wa mambo yao kuzikanya neema za Mwenyezi Mungu alizo wapa. Basi enyi makafiri mnao kataa! Stareheni kama mpendavyo. Mtakuja ujua mwisho wenu.

35 Kwani tuliwaacha katika upotovu wao, wala hatukuwazindua na ndoto zao, bali tukawateremshia hoja ya kushuhudia kwa yale walio kuwa wakiyashirikisha na Mwenyezi Mungu?

36 Na tukiwaonjesha watu neema huifurahia kwa furaha ya kuwatia kiburi. Na ikiwapata shida kwa madhambi waliyo yachuma wenyewe huwa wepesi wa kukata tamaa na Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema.

37 Je! Wameingiwa na ujinga hata hawajui nini kinacho fikisha kwenye Imani? Wala hawajui kwamba Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye, na humdhikisha amtakaye, kwa mujibu inavyo wafikiana na hikima yake? Hakika katika hayo zipo dalili wazi kwa watu wanao iaini Haki.

38 Na ilivyo kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye anaye kunjua riziki na akaidhikisha, basi mpe aliye jamaa haki yake kwa ajili ya hisani na kuunga udugu. Na mhitaji na aliye katikiwa safari yake wape pia haki zao kutokana na Zaka na Sadaka. Hayo ndiyo ya kheri kwa wenye kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, na wanataka thawabu zake. Na hao ndio wenye kufuzu kuipata neema ya milele.

39 Na mnacho toa, enyi wala riba, katika mali ili yakuzidieni kutokana na mali yao, basi kwa Mwenyezi Mungu hakizidi wala hakiingii baraka. Na mnacho toa sadaka kwa kutafuta wajiji wa Mwenyezi Mungu, bila ya riya, kujionyesha tu, wala tamaa ya kulipwa - basi hao ndio watakao pewa malipo mema marudufu.

40 Mwenyezi Mungu, *Subhanahu*, Aliye takasika, ndiye aliye kuumbeni. Kisha akakupeni cha kukupeni maisha. Kisha ndiye anaye kufisheni; na kisha atakufufueni kutoka makaburini kwenu. Je! Yupo yeyote katika hao miungu wa kishirikina mnao dai, na mkawaabudu badala ya Mwenyezi Mungu, mwenye kutenda hayo, ya kuumba, na kuruzuku, na kufisha, na kufufua, au kitendo chochote? Mwenyezi Mungu ametakasika na hayo wanayo mshirikisha naye.

41 Kumetokea moto, na ukame, na kila maafa, na kuharibika biashara, na mafuriko, kwa sababu ya uovu na madhambi, ili Mwenyezi Mungu awaadhibu watu duniani kwa baadhi ya vitendo vyao, huenda labda wakatubia maasi yao.

42 Ewe Nabii! Waambie washirikina: Nendeni pande mbali mbali za dunia, muangalie vipi waliishia

43. Basi uelekeze uso wako kwenye Dini Iliyo Nyooka kabla ya kufika Siku hiyo isiyo zuilika, inayo toka kwa Mwenyezi Mungu. Siku hiyo watu watatengana.⁴³
44. Anaye kufuru basi ukafiri wake utakuwa juu yake mwenyewe, na anaye tenda mema, basi wanazitengezea nafsi zao.⁴⁴
45. Ili awalipe walio amini na wakatenda mema kutokana na fadhila yake. Hakika Yeye hawapendi makafiri.⁴⁵
46. Na katika Ishara zake ni kuzituma pepo ziletazo bishara njema, na ili kukuonjesheni baadhi ya rehema zake, na ili majahazi yende kwa amri yake; na mtafute kutokana na fadhila yake, na ili mumshukuru.⁴⁶
47. Na hakika tulikwisha watuma Mitume kwa kaumu zao, na wakawajia kwa hoja zilizo wazi. Tukawaadhibu wale walio fanya ukosefu. Na ilikuwa ni haki juu yetu kuwanusuru Waumini.⁴⁷
48. Mwenyezi Mungu ndiye anaye zituma pepo zikayatimua mawingu, kisha akayatandaza mbinguni kama apendavyo. Na akayafanya mapande mapande, basi ukaiona mvua inatoka ndani yake. Anapo wafikishia awatakao katika waja wake, mara hao huwa na furaha.⁴⁸
49. Na ingawa kabla ya kuteremshiwa walikuwa wenye kukata tamaa.⁴⁹
50. Basi ziangalie athari za rehema ya Mwenyezi Mungu, jinsi anavyo ihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Basi hakika huyo ndiye bila ya shaka Mwenye kuhuisha wafu. Na Yeye ni Muweza wa kila kitu.⁵⁰

walio kutangulieni? Mtaona kuwa Mwenyezi Mungu aliwaangamiza na akayaharibu majumba yao, kwa sababu wengi walikuwa washirikina kama nyinyi.

43 Na uelekeze sawa sawa uso wako kwenye Dini iliyo kamilika kunyooka kwake, kabla haijafika Siku ambayo hapana mtu atakaye weza kuirejesha kwa Mwenyezi Mungu. Siku hiyo watu watagawanyika, na hali zao zitakhitalifiana.

44 Mwenye kumkufuru Mwenyezi Mungu, basi itampata mwenyewe laana ya ukafiri wake. Na wenye kuamini na wakatenda mema basi ni kwa ajili ya nafsi zao tu, wanajitengenezea njia nzuri iliyo nyooka.

45 Kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu huwalipa walio amini na wakatenda mema kwa yale walio yatanguliza. Na tena huwazidishia malipo yao kwa kuwafadhili. Kwani Yeye anawapenda hao na anawachukia walio kufuru na wakazikanya neema zake.

46 Na katika dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu na rehema yake ni kuwa Yeye huzipeleka pepo za kubashiria mvua kwa sababu ya kumwagia mashambani na kunyweshea wanyama na watu. Na ili akupeni katika kukumimieni hisani zake manufaa yanayo tokana na mvua, na ili zipate kwenda marikebu za majini kwa amri ya Mwenyezi Mungu na kudra yake, na ili mtafute riziki kwa fadhila yake kwa biashara na kutumia viliomo nchi kavu na baharini, na ili mpate kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ut'iifu wenu na kumuabudu Yeye tu.

47 Na kabla yako hakika tulikwisha watuma Mitume kwa kaumu zao. Na kila Mtume alikuja na hoja zilizo wazi, zenye kuonyesha ukweli wake. Kaumu yake ikamkadhibisha. Nasi, basi, tukawaangamiza wale walio fanya madhambi na wakaasi. Na Mwenyezi Mungu amejilazimisha nafsi yake kuwanusuru waja wake Waumini.

48 Mwenyezi Mungu, *Subhanahu* Wataa'la, Aliye takasika na akatukuka, ndiye anaye zituma pepo ambazo kwa nguvu zake zikayasukuma mawingu. Na Mwenyezi Mungu akayatandaza mbinguni kama atakavyo hapa na kule, kwa uchache au wingi. Na akayafanya mapande mapande. Basi nawe ndio unaona mvua inatoka kwenye mawingu. Na Mwenyezi Mungu anapo iteremsha mvua kwa waja wake awatakao, hao huwa wepesi kukunjuka roho na kufurahi. (Rejea kwenye maelezo ya Aya ya 43 ya Sura 24, An-Nur).

49 Nao hakika kabla ya kunyweshewa na mvua hiyo walikuwa wamekwisha kata tamaa na wamedawaa. 50 Basi iangalie mvua, muangalio wa kufikiri na kuzingatia, vipi Mwenyezi Mungu anavyo ihuisha ardhi baada ya kuwa imetulia kama maiti. Hakika aliye ihuisha ardhi baada ya kufa kwake bila ya shaka ni Muweza wa kuwahuisha watu. Na Yeye ni mtimilivu wa uweza, hashindwi na kitu.

- 51.** Na tunge utuma upepo na wakauona umekuwa rangi ya manjano, juu ya hayo wange endelea kukufuru.⁵¹
- 52.** Kwani wewe hakika huwafanyi maiti wakasikia, wala viziwi wakasikia wito wakisha geuka kukupa mgongo.⁵²
- 53.** Wala wewe huwaongoi vipofu na upotovu wao. Huwasikilizishi ila wanao ziamini Aya zetu. Hao ndio Waislamu, walio nyenyekea.⁵³
- 54.** Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni kutokana na udhaifu kisha akajaalia nguvu baada ya unyonge, kisha akajaalia baada ya nguvu unyonge tena na ukongwe. Anaumba atakavyo. Naye ndiye Mjuzi, Mwenye uweza.⁵⁴
- 55.** Na siku itapo simama Saa wakosefu wataapa kwamba hawakukaa duniani ila saa moja tu. Hivyo ndivyo walivyo kuwa wakipotozwa.⁵⁵
- 56.** Na walio pewa ilimu na Imani watasema: Hakika nyinyi mlikwisha kaa katika hukumu ya Mwenyezi Mungu mpaka Siku ya kufufuliwa. Basi hii ndiyo Siku ya kufufuliwa! Lakini nyinyi mlikuwa hamuijui.⁵⁶
- 57.** Basi Siku hiyo hautawafaa walio dhulumu udhuru wao, wala haitotakiwa toba yao.⁵⁷
- 58.** Na hakika tulikwisha wapigia watu kila mfano katika hii Qur'ani. Na ukiwaletea Ishara yoyote hapana shaka walio kufuru watasema: Nyinyi si chochote ila ni waongo.⁵⁸
- 59.** Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo piga muhuri kwenye nyoyo za wasio jua.⁵⁹

51 Nami ninaapa! Lau kuwa tukiwapeleka upepo wa kudhuru mimea, nao wakauona umekuwa manjano kwa sababu yake, hapana shaka wataendelea hata baada ya kuwa manjano, wakizikanya neema, na wakimkataa Mwenyezi Mungu.

52 Basi wewe usihuzunike kwa inadi yao na kuto kukuitikia. Kwani wewe huwezi kuwafanya maiti wausikie wito wako; wala kuwafanya viziwi wakusikie unapo wanadia, wakizidi uziwi wao kwa wanavyo kukimbia kwa mapuuzi.

53 Na watu hawa ni kama vipofu, kwa vile nyoyo zao zimefungika hawafuati uwongofu. Na wewe huwezi kuwaongoa vipofu, na ukawazuia wasifanye ukafiri wao. Ama hakika wewe unaweza kuwafanya wakusikie msikio wa kufahamu na kukubali wale ambao nyoyo zao zimejitayarisha kupokea Imani. Basi hao wanaifuata Haki inapo dhihiri.

54 Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni kutokana na tone la manii, mkawa dhaifu, hamna nguvu. Kisha akakujaalieni baada ya unyonge huo mkawa na nguvu. Akakukuzeni hata mkawa watu wazima. Kisha akakufanyeni baada ya nguvu hizi mkawa na udhaifu wa uzee na ukongwe. Yeye huumba atakavyo. Na Yeye ndiye Mjuzi wa kupanga uumbaji wake, Muweza wa kuleta atakacho.

55 Na Siku itapo fika Saa ya Kiyama makafiri wataapa kwamba hawakukaa duniani au makaburini mwao isipo kuwa kwa muda wa saa moja tu. Na mfano wa mwendo kama huo ndivyo Mashetani walikuwa wakiwaendesha duniani, kuwaachisha Haki na kuwapeleka kwenye upotovu.

56 Na walio pewa ujuzi na Mwenyezi Mungu, nao ni Manabii, na Malaika, na Waumini, watasema: Bila ya shaka nyinyi mlikwisha kaa katika hukumu ya Mwenyezi Mungu na amri yake mpaka Siku ya kufufuliwa. Basi hii ndiyo Siku ya kufufuliwa mlio ikanya. Na lakini nyinyi duniani mlikuwa hamjui kama hii ni Haki, kwa ujinga wenu na mapuuzi yenu.

57 Basi Siku hiyo watafufuliwa watu. Hakutowafaa kitu makafiri kutoa udhuru wao kwa kukanya kwao na kuwakadhibisha kwao Mitume wao. Wala hatawataka mtu yeyote wafanye jambo la kumridhi Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa wao wamekwisha dharaulika mbele yake, na wamefukuzwa kutokana na rehema yake.

58 Na kwa ajili ya uwongofu wa watu, tumebainisha katika Qur'ani hii kila mfano wa kuwaongoza kwenye Njia ya Uwongofu. Na wewe ukiwaletea kila muujiza bila ya shaka makafiri, kwa kupita hadi inda yao na ugumu wa nyoyo zao, watasema: Wewe na hao wanao kufuata si chochote ila ni waongo tu katika huo wito wenu.

59 Na muhuri kama huu umepigwa juu ya nyoyo za hao wasio ijua Tawhidi miongoni mwa majaahili.

60. Basi subiri. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya haki. Wala wasikupaparishe hao wasio kuwa na yakini.⁶⁰

60 Ewe Nabii, yavumilie maudhi yao. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu kukupa ushindi juu ya maadui wako, na kushinda kwa Uislamu juu ya dini zote, ni kweli isiyo geuka kabisa. Wala wasio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake wasikuletee dhiki na ukaiacha subira.

Sura 31 - Luqman

Utangulizi

Imeanza Sura hii tukufu kwa kueleza khabari za hichi Kitabu na uwongofu na rehema ziliomo ndani yake. Na wamesifiwa watu wema kwa kuwa wana ut'iifu kwa Mwenyezi Mungu, na wanaiamini Akhera, na watapata mafanikio. Na kinyume cha hayo yametajwa ya walio potea, wenye kiburi. Na wamebashiriwa Waumini kuwa watapata malipo mazuri katika makaazi ya Peponi. Na macho yanatakiwa yaangalie Ishara za ulimwengu zinazo onyesha uweza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na Upweke wake. Na Sura hii inawakabili makafiri kwa kuwaambia kwamba kwa hakika Mwenyezi Mungu wanaye muwekea washirika ameumba asicho kiweza yeyote asiye kuwa Yeye kukiumba. Tena Sura ikaingia kutaja wasia wa Luqman kumuusia mwanawe mausio yaliyo changanyika na mausio ya mtu na wazazi wake. Na ikaeleza mambo aliyo yat'iisha Mwenyezi Mungu kwa faida ya mwanaadamu, na neema zinazo onekana na zisio onekana alizo mjazia mwanaadamu.

Na ikaeleza khabari za wanao jadili mambo yaliyo mkhusu Mwenyezi Mungu bila ya ujuzi, na wanao toa udhuru kwa upotovu wao kuwa wanawafuata waliyo kuwa wakiyafuata baba zao. Na Sura ikamsifu anaye uelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu naye akawa ni mtenda mema, na ikamnasih Mtume asihuzunike kwa kukataa kwa mwenye kukufuru, kwani marejeo ya huyo ni kwa Mwenyezi Mungu. Na ikafafanua kwa wingi mambo yanayo onyesha uweza, na utukufu, na rehema.

Na Sura imeamrisha kumcha Mwenyezi Mungu, na kuogopa hisabu na malipo. Na imehadharisha ghururi, kudanganyika, na kumt'ii Shet'ani. Na ikakhitimisha kwa kutaja kuwa Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye ujuzi kamili wa kila kitu. Na muhimu ya iliyo kusanya Sura hii ni mambo matatu:

* Kwanza: Kuwabashiria watu wema kuwa watapata neema na furaha, na kuwaonya makafiri kuwa watapata adhabu.

* Pili: Kueleza Ishara za ulimwengu na mambo yaliyo wazi yenye kuonyesha uweza wa Mwenyezi Mungu, na Upweke wake, na upeo wa utukufu wake na rehema yake.

* Tatu: Wasia mkuu ulio kusudiwa usalama wa itikadi, na kulinda ut'iifu na tabia njema.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Mim (A.L.M.)¹
2. Hizi ni Aya za Kitabu chenye hikima.²
3. Kuwa ni Uwongofu na Rehema kwa wafanyao wema,³

1 Harufi hizi zimeanzia baadhi ya Sura kuashiria kuwa Qur'ani ni muujiza ulio tungwa na harufi kama harufi wanazo zitumia Waarabu katika maneno yao. Na juu ya hayo wao wameshindwa kuleta mfano wake. Na pia ni kwa ajili ya kuzindua watu wasikilize na watege sikio. Na washirikina walikuwa wamewafikiana kuwa wawe wanaropokwa maneno ya upuuzi tu ikisomwa Qur'ani wala wasisikilize.

2 Hizi Aya tukufu ni Aya za Qur'ani iliyo kusanya hikima na ukweli.

3 Hizi Aya ni Uwongofu ulio kamilika, na Rehema iliyo kusanya kwa wenye kutenda mema.

4. Wanao shika Sala, na wanatoa Zaka, nao wana yakini na Akhera.⁴
5. Hao ndio walio na uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi, na hao ndio wenye kufanikiwa.⁵
6. Na miongoni mwa watu wapo wanao nunua maneno ya upuuzi, ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu pasipo kujua, na wanaichukulia ni maskhara. Hao watapata adhabu ya kuwafedhehesha.⁶
7. Na (mtu kama huyo) anapo somewa Aya zetu huzipa mgongo kwa kujivuna, kama kwamba hakuzisikia, kama kwamba masikioni mwake mna uziwi. Basi mbashirie kuwa atapata adhabu chungu.⁷
8. Hakika walio amini na wakatenda mema watakuwa nazo Bustani za neema.⁸
9. Watadumu humo - ni ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kweli. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.⁹
10. Ameziumba mbingu bila ya nguzo mnazo ziona; na ameweka katika ardhi milima ili ardhi isikuyumbisheni; na ametawanya humo kila namna ya wanyama; na tumeteremsha maji kutoka mbinguni, na tukaotesha katika ardhi mimea mizuri ya kila namna.¹⁰
11. Huu ni uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Basi nionyeseni wameumba nini hao wasio kuwa Yeye! Lakini madhaalimu wamo katika upotovu uliyo dhaahiri.¹¹
12. Na tulimpa Luqman hikima, tukamwambia: Mshukuru Mwenyezi Mungu. Na mwenye kushukuru basi hakika anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake. Na aliye kufuru, basi Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Msifiwa.¹²
13. Na Luqman alipo mwambia mwanawe kwa kumpa mawaidha: Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu. Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhulma

4 Hao ndio wanao timiza Sala kwa njia ya ukamilifu kabisa, na wanawapa Zaka wanao istahiki; na wao wanayaamini maisha ya Akhera kwa imani yenye nguvu kabisa.

5 Hao Waumini wanao tenda vyema vitendo vyao, wametua kwenye Uwongofu ulio wajia kutokana na Mola wao Mlezi. Na hao tu - si wengineo - ndio wenye kufuzu kikweli.

6 Na miongoni mwa watu wapo ambao hununua maneno ya uwongo wawasimulie watu wapate kuwatenga na Uislamu na Qur'ani kwa kutojua dhambi zililo juu yao, na wanaifanyia maskhara Dini ya Mwenyezi Mungu na Ufunuo wake. Watendayo hayo watapata adhabu ya kuwatia unyonge na kuwadhalilisha.

7 Na mpotovu kama huyu akisomewa Aya za Mwenyezi Mungu huzipuuzi kwa kiburi. Hali yake kwa haya ni hali ya ambaye hasikii, kama kwamba ana uziwi katika masikio yake. Basi mwonye kuwa hakika Mwenyezi Mungu amemuandalia adhabu yenye machungu makali.

8 Hakika walio amini na wakatenda vitendo vyema watapata Bustani zenye neema.

9 Watabaki humo daima dawamu; Mwenyezi Mungu amewaahidi ahadi isiyo vunjika. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mshindi wa kila kitu, Mwenye hikima katika maneno yake na vitendo vyake.

10 Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu zisio na nguzo za nyinyi kuziona. Na juu ya ardhi ameweka milima iliyo simama imara, ili ardhi isikutingisheni. Na humo katika ardhi ametawanya kila namna ya wanyama wanao tambaa na kwenda. Na tumeteremsha maji kutoka mbinguni, na tukaotesha mimea ya kila namna nzuri yenye manufaa katika ardhi. (*Rejea uangalie maelezo ya kisayansi juu ya Aya 2, Sura ya 13, Ar-Raa'd*).

11 Hivi viumbe vya Mwenyezi Mungu vipo mbele yenu, basi hebu nionyeseni walicho umba hao mnoo wafanya ni miungu badala yake Yeye hata wawe ni washirika wake! Bali madhaalimu - kwa ushirikina wao - wamo katika upotovu ulio wazi.

12 Na hakika tulimpa Luqman hikima, na ilimu, na kauli ya kusibu. Tulimwambia: Mshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema aliyo kupa. Na mwenye kushukuru basi hakika huyo anaitafutia kheri nafsi yake. Na mwenye kuzikufuru neema, akazikataa, na asishukuru kwa ajili yake, basi kwa hakika Mwenyezi Mungu si mwenye kuihitaji shukra yake, na Yeye Mwenyezi Mungu ni Mwenye kustahiki sifa zote njema, na ingawa pasiwepo hata mmoja wa kumsifu.

iliyo kubwa.¹³

14. Na tumemuusia mtu kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili. (Tumemuusia): Nishukuru Mimi na wazazi wako. Ni kwangu Mimi ndiyo marudio.¹⁴

15. Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwa'ii. Lakini kaa nao kwa wema duniani, nawe ishike njia ya anaye elekea kwangu. Kisha marejeo yenu ni kwangu Mimi, na Mimi nitakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.¹⁵

16. Ewe mwanangu! Kikiwapo kitu cha uzito wa chembe ya khardali kikawa ndani ya jabali au ndani ya mbingu au ndani ya ardhi, basi Mwenyezi Mungu atakileta. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyo fichika, Mwenye khabari za yote.¹⁶

17. Ewe mwanangu! Shika Sala, na amrisha mema, na kataza maovu, na subiri kwa yanayo kupata. Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa.¹⁷

18. Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna na kujifakhirisha.¹⁸

19. Na ushike mwendo wa katikati, na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda.¹⁹

20. Kwani hamwoni ya kwamba Mwenyezi Mungu amevifanya vikutumikieni viliomo mbinguni na kwenye ardhi, na akakujalizieni neema zake, za dhaahiri na za siri? Na miongoni mwa watu wapo wanao bishana juu ya Mwenyezi Mungu pasipo ilimu, wala uwongofu, wala Kitabu chenye nuru.²⁰

13 Taja pale Luqman alipo mwambia mwanawe: Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu na yeyote. Hakika kumshirikisha Mwenyezi Mungu ni dhulma kubwa, kuwaweka sawa Mwenye kustahiki na asiye stahiki. (*Tazama Maelezo 31:13*)

14 Na tumemuamrisha mtu awafanyie wema wazazi wake, na mama yake ampe fungu kubwa zaidi. Kwani yeye alimbeba katika mimba kwa udhaifu unao zidi kila siku kidogo kidogo. Na tena kamnyonyesha muda wa miaka miwili ndipo alipo muachisha ziwa. Na tumemuusia: Mshukuru Mwenyezi Mungu na wazazi wako. Kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo kwa ajili ya hisabu na malipo.

15 Na ikiwa wazazi wako wakikushikilia kwa juhudi umshirikishe Mwenyezi Mungu na vitu usivyo vijua kuwa vinastahiki kuabudiwa, basi usiwakubalie. Lakini endelea na kusuhubiana nao duniani kwa wema na ihsani. Na fuata njia ya wanao rejea kwangu kwa Tawhidi, Imani ya Mwenyezi Mungu Mmoja, na Ikhlas, usafi wa niya na vitendo. Kisha nyote mtarejea kwangu, na nitakupeni khabari ya mliyo kuwa mkiyatenda, ya kheri na shari, ili nipate kukulipeni kwayo.

16 Ewe mwanangu! Hakika wema au ubaya kwa mtu, hata ukiwa, mathalan, kwa udogo wake kama chembe ya khardali, iliyoko pahali palipo fichikana kabisa, kama ndani ya jabali, au ndani ya mbingu, au chini ya ardhi, Mwenyezi Mungu ataufichua na autolee hisabu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyo fichika, hakifichikani kitu hata kidogo kwake, ni Mwenye khabari ya kujua hakika ya kila kitu.

17 Ewe mwanangu! Zihifadhi Sala, na amrisha kila wema, na kataza kila baya, na stahamili kwa shida zinazo kusibu. Hakika anayo usia Mwenyezi Mungu ni katika mambo ambayo yanahitajia kufanyiwa hima na kuyashikilia.

18 Wala usiwageuzie watu uso wako kwa takaburi, wala usitembee katika nchi kwa kujiona na majivuno. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila mwenye kuringa na kujiona.

19 Na nenda mwendo wa wastani, si mbio mbio mno wala taratibu mno. Na teremsha sauti yako. Kwani hapana sauti mbaya kama sauti ya punda. Inaanzia kwa mngurumo unao ghasi, na inaishia kwa ukenje unao kera.

20 Mmeona kwamba Mwenyezi Mungu amekudhalilishieni viliomo mbinguni kama jua, na mwezi, na nyota na vyenginevyo; na viliomo katika ardhi, kama mito, na matunda, na wanyama. Naye amekutimizieni neema zake zililo dhaahiri na zililo sitirika, msizo ziona. Na miongoni mwa watu, wapo wanao jadiliana juu ya dhiti ya Mwenyezi Mungu na sifa zake bila ya dalili wala uwongozi ulio pokewa kutokana na Nabii au Wahyi (ufunuo) wenye kumurika kwa mwangaza njia ya Haki

21. Na wanapo ambiwa: Fuateni aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, husema: Bali tunafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je! Ijapo kuwa Shet'ani anawaita kwenye adhabu ya Moto uwakao?²¹
22. Na mwenye kuuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekwisha kamata fundo lilio madhubuti. Na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu.²²
23. Na anaye kufuru, isikuhuzunisha kufuru yake. Kwetu ndio marudio yao, na hapo tutawaambia waliyo yatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.²³
24. Tunawastarehesha kwa uchache, kisha tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.²⁴
25. Na ukiwauliza: Nani aliye ziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Wewe sema: *Alhamdulillah!* Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui.²⁵
26. Ni vya Mwenyezi Mungu vyote viliomo mbinguni na katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi, Mwenye kusifiwa.²⁶
27. Na lau kuwa miti yote iliyomo duniani ikawa ni kalamu, na bahari (ikawa wino), na ikaongezewa juu yake bahari nyengine saba, maneno ya Mwenyezi Mungu yasingeli kwisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.²⁷
28. Hakukuwa kuumbwa kwenu, wala kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.²⁸

21 Na pindi wakiambiwa: Fuateni Haki na Uwongofu alio uteremsha Mwenyezi Mungu, wao husema: Bali sisi tunafuata tuliyo wakuta nao baba zetu. Je! Wanawafuata hao, ijapo kuwa Shetani ndio anawaita wende kwenye upotovu utakao waingizia Motoni?

22 Na mwenye kuuelekeza Mwenyezi Mungu kwa moyo wake na uso wake, na akamwakilisha Yeye mambo yake yote, naye akawa ni mwenye kutenda vitendo vyema, basi amefungamana na sababu za nguvu kabisa za kumfikisha kwenye radhi ya Mwenyezi Mungu. Na kwake Yeye, *Subhanahu*, ndio marejeo ya mambo yote.

23 Na asiye mtakasia Mwenyezi Mungu dhati yake na nafsi yake, basi usikuhuzunisha upinzani wake na mapuza yake. Kwetu Sisi peke yetu ndio marejeo yao Siku ya Kiyama. Hapo tutawaonyesha vitendo vyao. Kwani Sisi tumezunguka kwa kuvijua viliomo ndani ya nafsi zao, seuze vitendo vyao vya dhaahiri.

24 Tunawastarehesha kwa muda mchache katika dunia yao, kisha tutawalazimisha kwenda kwenye adhabu kali isiyo stahimilika.

25 Ewe Nabii! Nakuapia ya kuwa ukiwauliza: Nani aliye umbu mbingu na ardhi? Hapana shaka watasema: Ni Mwenyezi Mungu. Sema: Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, aliye ziweka dalili za Upweke wake hata zikaubomoa ushirikina wao wa kumshirikisha na wenginewe katika ibada. Na lakini wengi wao hawajui ya kuwa kwa kukiri kwao huku, basi wamesimamisha hoja ya kuwapinga wenyewe kwa ubovu wa itikadi yao.

26 Viliomo katika mbingu na ardhi ni vya Mwenyezi Mungu, kwa kuviumba, na kuvikadiria, na kuvipanga. Basi vipi wao wanaacha kumuabudu Yeye? Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika si mhitaji wa viumbe vyake wala ibada yao. Yeye ni Msifiwa kwa dhati yake. Ni mwenye kustahiki kusifiwa na waja wake.

27 Na lau kuwa miti yote ya duniani ikageuka kalamu, na maji yote ya baharini kwa wingi wake yakageuka wino, kuandikia maneno ya Mwenyezi Mungu, basi zingeli kwisha kalamu na wino ukamalizika kabla ya kumalizika maneno ya Mwenyezi Mungu. Kwani hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, hashindwi na chochote, Mwenye hikima hakimfutu kitu katika ujuzi wake na hikima yake. Basi hayeshi maneno yake na hikima yake.

28 Kukuumbeni nyinyi hapo mwanzo na kukufufueni baada ya kufa, mbele ya uweza wa Mwenyezi Mungu si chochote ila ni kama kumuumba na kumfufua mtu mmoja tu. Hakika Mwenyezi Mungu anaisikia kauli ya washirikina wanapo sema ati: Hakuna kufufuliwa. Naye ni Mwenye kuviona vitendo vyao, naye atawalipa kwavyo.

29. Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu huingiza usiku katika mchana, na huingiza mchana katika usiku, na amedhalilisha jua na mwezi? Vyote hivyo vinakwenda mpaka wakati ulio wekwa. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.²⁹

30. Hivi ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu ndiye wa kweli, na hakika wanacho kiomba ni cha uwongo. Na kwamba hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mtukufu na ndiye Mkubwa.³⁰

31. Kwani huoni kwamba marikebu hupita baharini zikichukua neema za Mwenyezi Mungu, ili kukuonyesheni baadhi ya Ishara zake? Hakika katika haya zipo Ishara kwa kila mwenye kusubiri, mwenye kushukuru.³¹

32. Na wimbi linapo wafunika kama wingu, wao humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia dini. Lakini anapo waokoa wakafika nchi kavu, wapo baadhi yao huenda mwendo wa sawa. Wala hazikanushi Ishara zetu ila aliye khaini kafiri mkubwa.³²

33. Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi, na iogopeni siku ambayo mzazi hatamfaa mwana, wala mwana hatamfaa mzazi kwa lolote. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala asikudanganyeni na Mwenyezi Mungu mdanganyifu.³³

34. Hakika kujua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye ndiye anaye iteremsha mvua. Na anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi. Na haijui nafsi yoyote itachuma nini kesho. Wala nafsi yoyote haijui itafia nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua, Mwenye khabari.³⁴

29 Je! Huangalii, ewe mwenye jukumu, kwa maangalio ya mwenye kuzingatia, ya kwamba hakika Mwenyezi Mungu huupunguza wakati wa usiku kwa kadri ya anavyo uongeza mchana? Na anaupunguza mchana kwa kadri ya anavyo uzidisha usiku? Naye amedhalilisha jua na mwezi kwa ajili ya maslaha yenu, na amefanya hayo yafuate mpango wa peke yao. Basi kila moja katika hayo huenda katika njia maalumu ya mbinguni wala haigeuki. Na mwendo huo unaendelea mpaka Siku ya Kiyama. Na hakika Yeye, *Subhanahu*, anazo khabari za yote myatendayo, na ni Mwenye kukulipeni kwayo

30 Hayo yaliyo tajwa ni katika ajabu za uundaji wa Mwenyezi Mungu na uweza wake, kwa sababu muundaji wake ni Mungu aliye thibiti Ungu wake, Mwenye kustahiki peke yake kuabudiwa, na kwamba miungu yote mnayo iabudu badala yake ni miungu ya uwongo. Na hakika Mwenyezi Mungu, peke yake, ndiye Mtukufu wa shani, Mkubwa wa utawala.

31 Ewe mtu! Huzitazami marikebu, vyombo vinavyo kwenda baharini kwa rehema ya Mwenyezi Mungu, vikichukua ndani yake bidhaa za kukupeni manufaa, ili Mwenyezi Mungu akuonyesheni baadhi ya maajabu ya uundaji wake, na dalili za uweza wake? Hakika katika hayo zimo Ishara kwa kila mwenye kuvumilia mitihani yake, mwenye kuzishukuru kwa neema zake.

32 Hawa makafiri wanao mkataa Mwenyezi Mungu wakipanda marikebu, na bahari ikawachafukia, na mawimbi yakaja juu mpaka wakaona yatawafunika, na wakawa yakini watazama bila ya muhali, humkimbilia Mwenyezi Mungu, wakimwomba kwa ikhlasi na unyenyekevu, awaokoe. Basi akisha waokoa wakafika nchi kavu wapo kati yao wachache wanao kumbuka ahadi yao, na wakenda mwendo wa sawa. Na wapo kati yao, nao ndio wengi, walio sahadu fadhila za Mola wao Mlezi, na wakaendelea na kumkataa. Na wala hakatai fadhila za Mola wake Mlezi na hisani yake ila kila mtu aliye mwingi wa ukhaini, aliye pita mpaka kumkanya Mola wake Mlezi.

33 Enyi watu! Fanyeni aliyo kuamrisheni Mola wenu Mlezi, na wacheni aliyo kukatazeni. Na tahadharini na adhabu yake ya Siku ya Kiyama, Siku ambayo kwamba mzazi hatamfaa mwanawe kwa lolote, wala mwana hatamfaa mzazi wake kwa lolote. Hakika Siku hii ndiyo aliyo iahidi Mwenyezi Mungu. Na ahadi yake ni ya kweli, hayendi kinyume. Basi yasikupumbazeni mapambo ya dunia na uzuri wake, mkaacha kujitayarisha kwa ajili ya Siku hiyo. Wala msikhadaiki na uchochezi wa Shetani, ukakuachisheni kumuelekea Mwenyezi Mungu na kumt'ii.

34 Hakika ujuzi wa Saa ya Kiyama uko kwa Mwenyezi Mungu umethibiti. Basi hapana anaye ijua isipo kuwa Yeye tu. Na Yeye huteremsha mvua kwa wakati wake alio uweka. Na anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi, kama wanaume, au wanawake, hivyo viliomo vimetimia au havikutimia mimba. Wala hapana mtu ajuaye, mwema na muovu, atapata nini kesho, kama kheri au shari. Wala hapana mtu ajuaye pahala gani duniani itamfika ajali yake ya kufa. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliye timia ujuzi wake na kuwa na khabari ya kila kitu. Wala hapana yeyote awezaye kujua siri yake.

Sura 32 - Assajdah

Utangulizi

Sura hii iliteremka baada ya Surat Al Muuminun. Nayo imekusanya mazungumzo juu ya kuteremshwa Kitabu, na umuhimu wa Mtume s.a.w., na kuumbwa mbingu na ardhi, na shani yake Mtukufu katika kupanga, na kumlea na kumuendeleza kumuumba mwanaadamu, na maneno ya wenye kukanya kufufuliwa na jawabu ya kuwajibu, na hali ya wakosefu Siku ya hisabu, na msimamo wa Waumini wakati zinapo tajwa Aya, na kubainisha malipo ya Waumini na waovu, na kuteremshiwa Musa a.s. Taurati, na vipi alivyo waamili Mwenyezi Mungu Wana wa Israili, na kuwaelekeza makafiri wa Makka wazingatie walivyo angamia walio watangulia, na kuwataka watazame kwa macho yao ili waamini kufufuliwa. Na Sura imetaja vipi hao makafiri walivyo ifanyia kejeli siku ya ushindi, na jawabu walio pewa.

Na lengo muhimu la Sura hii ni kuelekeza nadhari kwenye Ishara za ulimwengu ulivyo umbwa, na mazungumzo juu ya kufufuliwa, na jawabu za kuwarudi hao wanao kanya kufufuliwa, na kuwaelekeza makafiri wazingatie maangamizo yaliyo wasibu walio watangulia.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alif Lam Mim (A.L.M.)¹
2. Huu ni mteremsho wa Kitabu kisicho kuwa na shaka yoyote kinacho toka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.²
3. Au wanasema: Amekizua? Bali hichi ni Kweli iliyo toka kwa Mola wako Mlezi ili uwaonye watu wasio fikiwa na mwonyaji kabla yako; huenda wakaongoka.³
4. Mwenyezi Mungu ndiye aliye umba mbingu na ardhi na viliomo baina yao kwa siku sita, na akatawala kwenye Kiti cha Enzi. Nyinyi hamna mlinzi wala mwombezi isipo kuwa Yeye tu. Basi, je, hamkumbuki?⁴
5. Anapitisha mambo yote yalio baina mbingu na ardhi, kisha yanapanda kwake kwa siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu kwa mnavyo hisabu nyinyi.⁵

1 Alif Lam Mim, ni harufi zilizo undiwa Qur'ani, kama yalivyo undiwa maneno yenu. Ikiwa mmeshindwa kuleta mfano wake hii, basi ni ushahidi kuwa hii inatokana na Mwenyezi Mungu, wala hakuisema mwanaadamu.

2 Huu ni uteremsho wa Qur'ani umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote. Na Yeye ndiye mwenye kupanga mambo yao. Hapana shaka yoyote kuwa hii imeteremka kutoka kwake.

3 Ati wanasema: Kaizua Muhammad, naye akamsingizia Mwenyezi Mungu! Haiwafalii wao kusema hayo. Kwani hii ni Haki, Kweli, iliyo teremka kutokana na Mola wako Mlezi, ili upate kuwakhofisha kwayo watu ambao hawajapata kujiwa na Mtume kabla yako, utaraji kwa onyo hili wapate kuongoka na waifuate Haki.

4 Mwenyezi Mungu aliye umba mbingu na ardhi na vilio baina yao kwa siku sita, kisha akatawala juu ya Kiti cha Enzi, *A'rshi*, kwa utawala ulio laiki naye. Nyinyi hamna badala yake Yeye yeyote msaidizi wa kukunusuruni, wala mwombezi wa kukuombeeni. Basi je, mtaendelea kushikilia kuwa katika ukafiri na inda, wala msiwaidhike kwa mawaidha ya Mwenyezi Mungu?

5 Yeye huyaendesha mambo ya uumbaji katika mbingu na ardhi, kisha amri yake hupanda kwenda kwake

6. Huyu ndiye Mwenye kuyajua yasiyo onekana na yanayo onekana. Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.⁶
7. Ambaye ametengeneza vizuri umbo la kila kitu; na akaanzisha kumuumba mtu kwa udongo.⁷
8. Na kisha akajaalia uzao wake utokane na kizazi cha maji madhaifu.⁸
9. Kisha akamtengeneza, na akampulizia roho yake, na akakujaalieni kusikia na kuona, na nyoyo za kufahamu. Ni uchache mnavyo shukuru.⁹
10. Nao husema: Tutapo kwisha potea chini ya ardhi, ni kweli tutarudishwa katika umbo jipya? Bali wao wanakanusha kwamba watakutana na Mola wao Mlezi.¹⁰
11. Sema: Atakufisheni Malaika wa mauti aliye wakilishwa juu yenu; kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu Mlezi.¹¹
12. Na ungeli waona wakosefu wanvyo inamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao Mlezi, (wakisema): Mola wetu Mlezi! Tumesha ona, na tumesha sikia. Turejeshe tukatende mema, kwani hakika sisi tumekwisha kuwa na yakini sasa.¹²
13. Na lau tungeli taka tunge mpa kila mtu uwongofu wake. Lakini imekwisha kuwa kauli iliyo toka kwangu : Kwa yakini nitaijaza Jahannamu kwa wote hawa, majini na watu.¹³
14. Basi onjeni kwa vile mliyvo usahau mkutano wa Siku yenu hii. Na Sisi hakika tunakusahauni. Basi onjeni adhabu ya milele kwa yale mliyo kuwa mkiyatenda.¹⁴
15. Hakika wanao ziamini Aya zetu ni hao tu ambao wakikumbushwa hizo, basi wao huanguka kusujudu, na humsabihi Mola wao Mlezi kwa kumhimidi, nao hawajivuni.¹⁵

kwa siku ambayo kadiri yake ni kama miaka elfu kwa mujibu wa miaka ya duniani mnayo ihisabu nyinyi.

6 Huyu ndiye aliye sifika kwa kuumba na kutawala na kupanga, Mwenye kuyajua ya ghaibu ya viumbe vyote na wanayo yaona, ambaye amri yake ni yenye kushinda, Mkunjufu wa rehema,

7 Aliye umbu kila kitu kwa ustadi, kwa mujibu wa inavyo hitajia hikima yake, na akaanza kumuumba mtu wa mwanzo kwa udongo,

8 Kisha akawafanya dhuriya zake wa namna mbali mbali kutokana na maji machache, dhaifu, yasiyo tamanika kwa kawaida. (*Tazama Maelezo 32:8*)

9 Kisha akamsimamisha na kumkuza, na akamtia ndani yake siri yake aliyo mkhusisha nayo, na akakupeni masikio, na macho, na akili, mpate kusikia na kuona na kufahamu. Nanyi hamshukuru ila kwa uchache.

10 Na wanao kanya kufufuliwa wakasema: Ati sisi tukisha kuwa mchanga, ulio changanyika na mchanga wa ardhi, usibagulike, ndio kweli tutarejea kwa umbo jipya? Hao hakika si kama wanakanya kufufuliwa tu, bali wanakadhibisha yote yatayo kuwako Akhera.

11 Sema: Atakufisheni Malaika wa mauti, aliyewakilishwa kuzikamata roho zenu utapo kwisha muda wenu. Kisha kwa Mwenyezi Mungu peke yake ndio mtarejea.

12 Lau kuwa umejaaliwa kuwaona wakosefu kwenye msimamo wa hisabu ungeli ona ajabu. Pale wale wakosefu wenye kujivuna watavyo inamisha vichwa vyao kwa hizaya inayo tokana na Mola wao Mlezi, nao watasema kwa unyonge: Ewe Mola wetu Mlezi! Tumekwisha yaona tuliyo kuwa na upofu nayo, na tumekwisha yasikia tuliyo kuwa na uziwi nayo, basi turejeshe duniani tupate tenda mema ambayo tuliyo kuwa hatuyatendi. Hakika sasa hivi sisi tumeyakinika na walio kuja nayo Mitume wako.

13 Na lau kuwa tunataka tungeli mpa kila mtu uwongofu wake, lakini kauli yangu ilikwisha tangulia, nayo ni: Bila ya shaka nitaijaza Jahannamu kwa wote hawa majini na watu. Kwa kuwa tulijua kuwa wengi wao watakiari upotovu

14 Basi ionjeni adhabu kwa vile mliyvo ghafulika na kukutana nami hii leo. Hakika Sisi tunakuacheni katika adhabu kama watu walio sahauliwa. Na onjeni adhabu ya milele isiyo katika, kwa sababu ya ukafiri wenu na uasi wenu.

15 Hakika wanazasadiki Ishara zetu wale ambao wanapo waidhiwa kwazo huanguka chini kwa kumsujudia Mwenyezi Mungu, na wakamtakasa Mola wao Mlezi na kila upungufu, na wakamsifu kwa kila ukamilifu. Na wala wao hawatakabari wakakataa kuzifuata Ishara hizi.

- 16.** Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyo waruzuku.¹⁶
- 17.** Nafsi yoyote haijui waliyo fichiwa katika hayo yanayo furahisha macho - ni malipo ya yale waliyo kuwa wakiyatenda.¹⁷
- 18.** Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa.¹⁸
- 19.** Ama walio amini na wakatenda mema, watakuwa nazo Bustani za makaazi mazuri. Ndio pa kufikia kwa waliyo kuwa wakiyatenda.¹⁹
- 20.** Na ama wale walio tenda uovu, basi makaazi yao ni Motoni. Kila wakitaka kutoka humo watarudishwa humo humo. Na wataambiwa: Onjeni adhabu ya Moto ambayo mliyo kuwa mkiikanusha.²⁰
- 21.** Na tutawaonjesha adhabu khafifu kabla ya adhabu kubwa, huenda labda watarejea.²¹
- 22.** Na ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye kumbushwa kwa Ishara za Mola wake Mlezi, kisha akazikataa? Hakika Sisi tutajilipiza kwa wakosefu.²²
- 23.** Hakika Sisi tulikwisha mpa Musa Kitabu. Basi usiwe na shaka kuwa kakipokea. Na tukakifanya kuwa ni uwongofu kwa Wana wa Israili.²³
- 24.** Na tukawafanya miongoni mwao waongozi wanao ongoa watu kwa amri yetu, walipo subiri na wakawa na yakini na Ishara zetu.²⁴
- 25.** Hakika Mola wako Mlezi ndiye atakaye fafanua baina yao Siku ya Kiyama katika waliyo kuwa wakikhitalifiana.²⁵
- 26.** Je! Haijawabainikia kwamba kaumu ngapi tuliziangamiza kabla yao, nao wanapita katika maskani zao hizo? Hakika katika hayo zipo Ishara. Basi, je, hawasikii?²⁶

16 Mbavu zao zinabambatuka na vitanda vyao, yaani wanaacha usingizi wao, kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa kuikhofu ghadhabu yake, na kutumai rehema yake; na ambao kutokana na mali tuliyo wapa wanatoa kwa ajili ya mambo ya kheri.

17 Na hapana mtu yeyote anaye jua kiasi cha Mwenyezi Mungu alichu muandalia na akawafichia katika neema kubwa kubwa, na ambazo ni za kupoza macho yao, kuwa ni malipo kwa waliyo kuwa wanayachuma ya ut'iifu na vitendo.

18 Kwani watu watakuwa sawa katika malipo yao, na hali wamekhitalifiana katika vitendo vyao? Je! Aliye kuwa mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu ni kama mwenye kumkataa na akamuasi? Hasha! Hawawi sawa!

19 Ama walio amini na wakatenda mema watapata Bustani za Utulivu ziwe ndio maskani zao, kuwa ni ukarimu watao kirimiwa kwa waliyo kuwa wakiyatenda.

20 Ama wale walio toka nje ya ut'iifu wa Mwenyezi Mungu kwa kufuru zao, makaazi yao aliyote watayarishia ni Motoni. Kila wakijaribu kutoka watarudishwa huko huko. Na wataambiwa: Onjeni adhabu ya Moto ambayo mlipo kuwa duniani mkishikilia kuikadhibisha.

21 Na tunaapa: Hapana shaka tutawaonjesha duniani adhabu duni kabla hawajaifikia hiyo adhabu kubwa kabisa, nayo ni kudumu milele katika Moto. Huenda pengine watakao adhibiwa kwa hiyo adhabu duni watatubia, waache ukafiri wao.

22 Na hapana mtu yeyote aliye zidi udhaalimu kuidhulumu Haki na kuidhulumu nafsi yake, kuliko mtu anaye kumbushwa kwa Ishara za Mwenyezi Mungu na hoja zilizo wazi, kisha akaacha kuziamini juu ya kuwa ni wazi dhaahiri. Hakika Sisi tutajilipiza juu ya kila mkosefu!

23 Na Sisi tulikwisha mpa Musa Taurati. Basi usiwe na shaka na kupokea kwa Musa Kitabu hicho. Na tumekijaalia Kitabu alichu teremshiwa Musa kiwe ni uwongofu kwa Wana wa Israili.

24 Na kutokana na Wana wa Israili tumekijaalia wawepo Maimamu, waongozi, wa Dini, wasimame kuwaongoa watu, kwa kuitikia amri yetu kwa vile walivyo vumilia kuyatenda yaliomo katika Taurati, na wakawa wanazisadiki Ishara zetu ukomo wa kusadiki.

25 Hakika Mola wako Mlezi ndiye peke yake atakaye hukumu baina ya Manabii na kaumu zao Siku ya Kiyama katika mambo wanayo khitalifiana.

26 Je! Kwani Mwenyezi Mungu aliwaacha walio wakadhibisha Mitume wao, na hakuwabainishia

27. Je! Hawaoni ya kwamba tunayapeleka maji kwenye ardhi kavu, kisha kwayo tunaitoa mimea wanayo kula wanyama wao na wao wenyewe? Je! Hawaoni?²⁷
28. Wanasema: Ushindi huu ni lini, kama mnasema kweli?²⁸
29. Sema: Siku ya Ushindi, wale walio kufuru imani yao haitawafaa kitu, wala wao hawatapewa muhula.²⁹
30. Basi wapuuze, nawe ngonja; hakika wao wanangoja.³⁰

kwamba Yeye aliwahilikisha wengi katika kaumu zilizo watangulia, na wao wanapita kwenye majumba yao, na wanatembea kwenye maskani zao? Hakika katika hayo pana mawaidha ya kuwaonyesha Haki. Wao wameingiwa na uziwi, hawasikii mawaidha haya.

27 Wameingia upofu, na wala hawaoni ya kwamba hakika Sisi tunapeleka mvua na mito kwenye ardhi za ukame ambazo hazime mimea, na tukaziotesha mazao yake, wakala wanyama wao, na wao wenyewe wakala nafaka zake na matunda yake? Wamepofuka, na kwa hivyo hawazioni dalili za Mwenyezi Mungu za kuwafufua wafu.

28 Na washirikina wanakwambia wewe na Waumini: Wakati gani Mwenyezi Mungu atakufungulieni mpate ushindi? Twambieni wakati wake ikiwa nyinyi ni wasema kweli.

29 Waambie: Siku ya hukumu na kufafanua ikikufikilieni, walio kufuru haitowafaa kitu imani yao, wala hawatapewa muhula hata chembe ya hiyo adhabu wanayo istahiki.

30 Na ikiwa kufanya maskhara kama hivi ndio mtindo wao, basi wapuuze mbali. Na wewe ngojea ukweli aliyo kuahidi Mola wako Mlezi juu yao, kwani wao wanakungojea ushindwe.

Sura 33 - Al-Ah'zab

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kumtaka Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. amche Mwenyezi Mungu na amtegemee Yeye. Tena ikaingia kuzungumza juu ya mas-ala ya watoto wa kupanga, na ikakataa kuwa hao wana wanao walea kuwa ni watoto wao khasa. Na ikataja mapenzi na ut'iifu wa Mwenyezi Mungu alio wajibisha kwa ajili ya Mtume wake, na hishima na kuwatukuza Mamama wa Waumini, yaani wake za Mtume. Na Sura imeeleza ahadi aliyo ichukua Mwenyezi Mungu kwa Manabii kuwa wafikishe ujumbe; na ikafafanua khabari za Vita vya Ah'zab (Makundi) na khofu na misukosuko iliyo kuwako, na vipi mwishoe Waumini wakashinda na ahadi ya Mwenyezi Mungu ikatimia. Na Sura hii ikashughulikia kutaja adabu ambazo zinawapasa wake za Mtume kuzifuata, na wajilazimishe nafsi zao kuzishika. Tena ikaangukia kuzungumza juu ya watoto wa kupanga, na ikavunja ada ya siku za kijahiliya, za ujinga, ilipo kuwa kuharimisha mtu kuoana na mwana wa kupanga ambaye kwa hakika ni halali yake. Na Sura ikamsifu Mtume s.a.w. na ikamthibitishia aliyo kuwa anastahiki. Na ikausia kustareheshwa na kumwacha kwa wema mwanamke anaye pewa talaka kabla ya kuingia harusi. Na ikamkhusisha Mtume s.a.w. kuwa imemhalalishia mwanamke aliye jitolea kuolewa naye, na ikasema wazi kuwa si halali kwake kuzidisha kuowa wanawake wengine baada ya hao tisa alio kuwa nao. Kisha Sura tukufu ikabainisha yanayo wajibikia Waumini kuyafuata wanapo ingia nyumba za Nabii kwa ajili ya kula, na kuwa wakisha wende zao, na juu ya kuwauliza wake zake nyuma ya pazia. Na Sura ikawataka Mamama wa Waumini (wake za Mtume s.a.w.) wateremshe mitandio yao juu ya vifua vyao. Na Sura ikazungumza juu ya Saa na vitisho vya Kiyama, na ikatoa nasaha ya kumcha Mwenyezi Mungu, na kusema maneno yaliyo sawa, na ikakhitimishia kwa kutaja jukumu la Mwenyezi Mungu alilo libeba mwanaadamu, hali mbingu na ardhi na milima ilishindwa kulibeba.

Kutokana na hayo inaonekana kuwa makusudio muhimu kabisa ya Sura hii ni: Maneno juu ya watoto wa kupanga, na kuiyunja ada iliyo kuwa imeenea wakati ule kuharimisha kuwaoa wana wa kupanga ambao ni halali kwao; na ihsani ya Mwenyezi Mungu kuwafanyia Waumini kwa ushindi kuwashinda washirikina kama alivyo waahidi; na kufafanua sharia aliyo wawekea Mwenyezi Mungu Waumini wanapo ingia nyumba za Nabii s.a.w. na kuwaharimishia kuwaoa wake zake baada yake, na kuzipanga adabu makhsusi zilizo wakhusu Mamama wa Waumini, yaani wake za Mtume s.a.w.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ewe Nabii! Mche Mwenyezi Mungu wala usiwat'ii makafiri na wanaafiki. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima.¹

¹ Ewe Nabii endelea hivyo hivyo, kama ulivyo, kumcha Mwenyezi Mungu, wala usiyakubali mawazo ya makafiri na wanaafiki. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuvizunguka vitu vyote kwa kuvijua, ni Mwenye hikima katika kauli yake na vitendo vyake.

2. Na fuata uliyo funuliwa kwa wahyi kutokana na Mola wako Mlezi. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari ya mnayo yatenda.²
3. Na mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa ni wa kutegemewa.³
4. Mwenyezi Mungu hakumwekea mtu yeyote kuwa ana nyoyo mbili ndani ya mwili wake. Wala hakuwafanya wake zenu - ambao mnawalinganisha migongo yao na migongo ya mama zenu - kuwa ni mama zenu. Wala hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa ni wana wenu khasa. Hayo ni maneno ya vinywa vyenu tu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anaye sema kweli, naye ndiye anaye ongoa Njia.⁴
5. Waiteni kwa baba zao, maana huo ndio uadilifu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na ikiwa hamwajui baba zao, basi ni ndugu zenu katika Dini, na rafiki zenu. Wala si lawama juu yenu kwa mlivyo kosea. Lakini ipo lawama katika yale ziliyo fanya nyoyo zenu kwa makusudi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁵
6. Nabii ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao. Na wake zake ni mama zao. Na jamaa ni karibu wao kwa wao katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu kuliko Waumini wengine na Wahamiaji. Ila muwe mnawafanyia wema marafiki zenu. Haya yamekwisha andikwa Kitabuni.⁶
7. Na tulipo chukua ahadi kwa Manabii na kwako wewe, na Nuhu na Ibrahim na Isa mwana wa Mariamu, na tulichukua kwao ahadi ngumu,⁷
8. Ili (Mwenyezi Mungu) awaulize wakweli juu ya ukweli wao. Na amewaandalia

2 Na fuata wahyi unao teremka juu yako kutokana na Mola wako Mlezi. Hakika Mwenyezi Mungu anaye kufunulia kwa wahyi anazo khabari hata za mambo madogo madogo unayo yatenda wewe, na wanayo yatenda makafiri na wanaafiki..

3 Na wewe mwachilie mambo yako yote Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anatosha kabisa kuwa ni mtegemewa wa kila jambo.

4 Mwenyezi Mungu hakumjaalia mtu yeyote kuwa ana nyoyo mbili ndani ya mwili wake; wala hakumfanya mke wa yeyote katika nyinyi kuwa ni mama yake, pale anapo sema ati: Wewe kwangu mimi kama mgongo wa mama yangu! Wala hakuwafanya watoto mnao wapanga kuwa ni wenenu, kuwa hakika ni wana wenu kwa nasaba. Hayo ya kuwafanya watoto wa kupanga kuwa ni wenenu, ni kauli inayo toka kwenye vinywa vyenu, wala hayana ukweli. Hapana hukumu yoyote inayo tokana na hayo. Na Mwenyezi Mungu anasema jambo lililo thibiti la hakika. Na anakuongozeni mlifikie. Na Yeye peke yake *Subhanahu* ndiye anaye ongoa watu kwenye Njia iliyo sawa.

5 Wanasibishieni hawa watoto kwa baba zao khasa. Hayo ndiyo ya uadilifu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Ikiwa hamwajui baba zao walio nasibiana nao khasa, basi hao ni ndugu zenu katika Dini na rafiki zenu wa kuwanusuru. Wala nyinyi hamna dhambi ikiwa mmewanasibisha na watu wasio kuwa baba zao kwa kukosea. Lakini inakuwa dhambi kwa mlilo kusudia kwa nyoyo zenu baada ya kwisha jua yaliyo. Na Mwenyezi Mungu anakusameheni kwa kukosea kwenu, na anaikubali toba yenu kwa makosa mliyo kusudia.

6 Nabii Muhammad ni mwenye kustahiki zaidi urafiki kwa Waumini, na ana huruma zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao. Basi yawapasa wao wampende na want'ii. Na wake zake ni Mama zao kwa kuwatukuza na kuwahishimu, na kuwa ni haramu juu yao kuwaoa baada yake. Na jamaa walio khusiana ni karibu zaidi kuliko Waumini wenginewe na Wahajiri, walio hama Makka, kwa kurithiana wao kwa wao kama ilivyo wajibika katika Qur'ani. Lakini inafaa kumfanyia wema mlilo fanya urafiki naye katika Dini asiye kuwa jamaa yenu, kwa kuwapa wema na mapenzi au hata kumuandikia mali katika wasia. Hayo ya kurithiana jamaa walio khusiana yamethibiti katika Kitabu cha Qur'ani wala hayawezi kubadilishwa.

7 Na kumbusha pale tulipo fanya agano na Manabii wote walio tangulia kuwa watafikisha ujumbe na wito kulingania Dini iliyo sawa, na wewe, na Nuhu, na Ibrahim, na Musa, na Isa bin Maryamu; na tukachukua kwao agano lenye shani kubwa.

makafiri adhabu chungu.⁸

9. Enyi mlio amini! Zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilio juu yenu. Pale yalipo kufikilieni majeshi, nasi tukayapelekea upepo, na majeshi msiyo yaona. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yatenda.⁹

10. Walipo kujieni kutoka juu yenu, na kutoka chini yenu; na macho yalipo kodoka, na nyoyo zikapanda kooni, nanyi mkamdhania Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali.¹⁰

11. Hapo ndipo Waumini walipo jaribiwa, na wakatikiswa mtikiso mkali.¹¹

12. Na walipo sema wanaafiki na wale wenye maradhi katika nyoyo zao: Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu tu.¹²

13. Na kundi moja katika miongoni mwao lilipo sema: Enyi watu wa Yathrib! Hapana kukaa nyinyi! Rudini. Na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume kwa kusema: Hakika nyumba zetu ni tupu. Wala hazikuwa tupu; hawakutaka ila kukimbia tu.¹³

14. Na lau kuwa wangeli ingiliwa kwa pande zote, kisha wakatakiwa kufanya khiana, wangeli fanya, na wasingeli sita ila kidogo tu.¹⁴

15. Na hakika walikwisha muahidi Mwenyezi Mungu kabla yake kwamba hawatageuza migongo yao. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuulizwa.¹⁵

16. Sema: Kukimbia hakukufaeni kitu ikiwa mnakimbia mauti au kuuwawa, na hata hivyo hamtastareheshwa ila kidogo tu.¹⁶

17. Sema: Ni nani wa kukulindeni na Mwenyezi Mungu pindi akikutakieni uovu, au akikutakieni rehema? Wala hawatapata mlinzi wala msaidizi isipo kuwa Mwenyezi

8 Ili Mwenyezi Mungu awaulize Manabii Siku ya Kiyama juu ya waliyo waambia kaumu zao. Na Yeye amewaandalia wenye kuwakataa Mitume adhabu yenye kutia uchungu.

9 Enyi mlio amini zikumbukeni neema na fadhila za Mwenyezi Mungu zilio juu yenu, pale yalipo kujieni makundi katika Siku ya Handaki. Tukawapelekea upepo mkali wa kimbunga ubaridi, na Malaika ambao nyinyi hamwaoni. Kikawaingia kiwewe katika nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu alikuwa Mwenye kuviona vitendo vyenu, na ukweli wa niya zenu. Basi akaingia kukulindeni.

10 Walipo kujieni kutoka upande wa juu ya bonde, na kutoka chini, na macho yakakodoka, na nyoyo zikapanda mpaka kwenye koo, kwa kufazaika na kubabaika. Na nyinyi katika wakati ule wa shida kubwa kila namna ya dhana zilikujiuoni juu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu. (*Tazama* Maelezo 33:10)

11 Katika wakati ule Waumini walifanyiwa mtihani juu ya kusubiri kwao juu ya Imani. Wakatikisika kwa khofu kwa mtikiso mkubwa.

12 Na kumbuka shaka iliyo waingia wanaafiki na wagonjwa wa nyoyo walipo sema: Ahadi aliyo tupa Mwenyezi Mungu na Mtume ni ahadi ya uwongo, imekusudiwa kutudanganya tu.

13 Na kumbuka walipo sema kikundi cha wanaafiki na ambao wanao rega rega: Enyi watu wa (Yathrib, yaani) Madina! Hapana maana kubakia hapa nyinyi katika vita hivi vya kushindwa. Rudini mwende makwenu. Na kundi jingine kati yao walimtaka ruhusa Mtume warejee Madina, na wakasema: Hakika nyumba zetu hazina ulinzi. Hatuna budi kurejea tukazilinde. Wala nyumba zao hazikuwa khatarini kabisa kama walivyo sema. Hawakutaka ila kukimbia vita tu, kwa udhuru wa uwongo.

14 Lau kuwa makundi ya majeshi ya maadui wangeli waingilia Madina kwa kila upande, na wakawataka watangaze kuwa wameuwacha Uislamu na wawapige vita Waislamu bila ya shaka wangeli wakubalia yale waliyo takiwa, na wala wasingeli sita ila muda mfupi tu.

15 Na hakika hawa wenye kukimbia kutoka midani ya vita walikwisha muahidi Mwenyezi Mungu kabla yake kuwa watasimama imara katika vita pamoja na Mtume, na wala hawatakimbia. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuulizwa kwa yule mwenye kuitoa, na yampasa aitimize.

16 Waambie: Kukimbia hakukufaeni kitu ikiwa ndio mnayakimbia mauti au kuuwawa, maadamu ajali yenu imekwisha fika. Na ikiwa haijafika, basi hamtobaki mkistarehe katika dunia ila kwa muda wa umri wenu, nao ni mchache.

Mungu.¹⁷

18. Kwa hakika Mwenyezi Mungu anawajua hao wanao zuilia, na wanao waambia ndugu zao: Njooi kwetu! Wala hawaingii vitani ila kidogo tu.¹⁸

19. Wana choyo juu yenu. Ikifika khofu utawaona wanakutazama na macho yao yanazunguka, kama yule ambaye aliye zimia kwa kukaribia mauti. Na khofu ikiondoka wanakuudhini kwa ndimi kali, nao ni mabakhili kwa kila la kheri. Hao hawakuamini, basi Mwenyezi Mungu amevibat'ilisha vitendo vyao. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.¹⁹

20. Wanafikiri yale makundi ya maadui hayajaondoka. Na yakija hayo makundi watatamani laiti wao wako majangwani pamoja na mabedui, wakiuliza khabari zenu. Na lau wakiwa pamoja nanyi hawapigani ila kidogo tu.²⁰

21. Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.²¹

22. Na Waumini walipo yaona makundi, walisema: Haya ndiyo aliyo tuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamesema kweli. Na hayo hayakuwazidisha ila Imani na ut'iifu.²²

23. Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.²³

24. Ili Mwenyezi Mungu awalipe wakweli kwa sababu ya ukweli wao, na awaadhibu

17 Waambie hawa wanao babaika: Nani atakaye kulindeni na Mwenyezi Mungu akitaka kukuleteeni shari, au atakaye kuzuieni msipate kheri, akitaka Yeye kukurehemuni? Wala hawatapata badala ya Mwenyezi Mungu yeyote wa kuwalinda au kuwaokoa.

18 Hakika Mwenyezi Mungu anawajua wanao zuilia miongoni mwenu, na wanao waambia ndugu zao: Unganeni nasi! Wala hawaingii katika vita vinapo shitadi ila kidogo tu.

19 Wana pupa juu yenu kwa kuonekana dhaahiri inapo kuwa hapana khofu. Na ikija khofu ya adui au ya Mtume s.a.w. utawaona wanakuangalia na macho yao yanawazunguka hawajitambui, kama hali ya mwenye kuzimia wakati wa sumbuko la kukaribia mauti. Na khofu ikiondoka wanapita mpaka kukutukaneni na kukushutumuni kwa ndimi za kukata. Hao ni mabakhili kwa kila la kheri. Hao hawakuamini kwa nyoyo zao, ijapo kuwa wametangaza kuwa ni Waislamu. Basi Mwenyezi Mungu amezibat'ilisha a'mali zao kwa ukafiri wao walio dhamiria. Na kubat'ilisha huko ni jambo jepesi kwa Mwenyezi Mungu. (*Tazama Maelezo 33:19*)

20 Wanadhani hawa wanaafiki kwamba majeshi ya makafiri yaliyo ungana bado yapo mahali pao wanaizinga Madina. Na hayo makundi ya maadui yakirejea tena, watatamani hao woga laiti wangu kuwa wanaishi pamoja na mabedui huko majangwani wakidondoa khabari zenu. Na lau wakibaki kwenye kambi zao, na wasikimbie, na majeshi mawili yakapambana, basi hata hivyo wasinge pigana pamoja nanyi ila kidogo tu, kama kujionyesha na watajwe kuwa nao walikuwamo.

21 Hakika nyinyi mna kiigizo kizuri kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kutaraji rehema ya Mwenyezi Mungu, na neema za Siku ya Mwisho, na akamkumbuka na kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi katika khofu na kutumai, na katika shida, na katika neema.

22 Na Waumini walipo yaona makundi ya washirikina walisema: Haya ndiyo aliyo tuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume wake zamani. Kwani walituahidi tutapata shida, na kisha tutapata ushindi. Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamesema kweli. Taabu hizi basi, hazikuwazidishia ila nguvu za kumuamini Mwenyezi Mungu, na uzuri wa kuinyenyekea kwao hukumu yake.

23 Miongoni mwa hawa Waumini wapo watu walio muahidi Mwenyezi Mungu kuwa watasimama imara na Mtume katika vita. Nao wakatimiza ahadi yao. Miongoni mwao wapo walio pata utukufu wa kufa mashahidi, na wengine wamebakia wahi walingojea nao kupata utukufu huo. Wala hawakuigeza ahadi ya Mwenyezi Mungu waliyo jikatia juu ya nafsi yao, wala hawakuigeza chochote katika hayo.

wanaafiki pindi akitaka, au apokee toba yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.²⁴

25. Na Mwenyezi Mungu aliwarudisha nyuma makafiri juu ya ghadhabu yao; hawakupata kheri yoyote. Na Mwenyezi Mungu amewatosheleza Waumini katika vita. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na uweza.²⁵

26. Na akawateremsha wale walio wasaidia (maadui) katika Watu wa Kitabu kutoka katika ngome zao; na akatia khofu katika nyoyo zao. Baadhi yao mkawa mnawauwa, na wengine mnawateka.²⁶

27. Na akakurithisheni ardhi zao na nyumba zao na mali zao, na ardhi msiyo pata kuikanyaga. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.²⁷

28. Ewe Nabii! Waambie wake zako: Ikiwa mnataka maisha ya dunia na pambo lake, basi njooni, nitakupeni kitoka nyumba, na kukuacheni mwachano mzuri.²⁸

29. Na ikiwa mnamtaka Mwenyezi Mungu na Mtume wake na nyumba ya Akhera, basi Mwenyezi Mungu amewaandalia wafanyao mema, miongoni mwenu, malipo makubwa.²⁹

30. Enyi wake wa Nabii! Atakaye fanya uchafu dhaahiri miongoni mwenu, atazidishiwa adhabu mara mbili. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.³⁰

31. NA MIONGONI mwenu atakeye mt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akatenda mema, tutampa malipo yake mara mbili, na tutamwandalia riziki ya ukarimu.³¹

32. Enyi wake wa Nabii! Nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine. Kama mnamcha Mungu basi msiregeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake. Na semeni maneno mema.³²

24 Ili Mwenyezi Mungu apate kuwalipa Waumini walio wakweli kwa sababu ya ukweli wao katika Imani yao na kutimiza kwao ahadi waliyo itoa. Na awaadhibu wanaafiki - pindi akitaka - au amwezesh aliye elekea, kufikia toba. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe kwa kukubali toba, Mwenye kurehemu kwa kusamehe maasi.

25 Mwenyezi Mungu akawarudisha nyuma makafiri walio jiunga makundi kumpiga Mtume na nyoyo zao zimejaa chuki. Hawakupata kheri yoyote kwa ushindi wala ngawira. Na Mwenyezi Mungu amewatosheleza Waumini wasipate mashaka, kwa kuwapatiliza wale makafiri kwa upepo na Malaika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza wa kutimiliza alitakalo, ni Mwenye nguvu hapana wa kumshinda.

26 Na Mwenyezi Mungu aliwateremsha walio wasaidia makundi ya maadui katika Watu wa Kitabu, nao ni Mayahudi wa Bani Quraidha, kutokana na ngome zao walipo kuwa wakijilinda ndani yake. Na akaingiza katika nyoyo zao kitisho. Wengine mkawa mnawawauwa, nao ni wanawake na watoto.

27 Na akakurithisheni ardhi zao, na nyumba zao, na mali zao, na ardhi ambazo nyayo zenu hazijapata kuzikanyaga kabla yake. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ni Muweza wa kutimiza kila alitakalo.

28 Ewe Nabii! Waambie wake zako kwa kuwanasihii: Ikiwa mnataka maisha ya duniani na starehe zake, basi jongoeni nitakupeni cha kupunguza upweke wa talaka, itakuwa ni tunza yenu. Na nitakupeni talaka isiyo na uovu ndani yake.

29 Na ikiwa mnakhiari mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na neema za nyumba ya Akhera, na mnaridhi maisha magumu mlio nayo hivi sasa, basi hakika Mwenyezi Mungu amewaandalia mfano wenu nyinyi miongoni mwa wanawake walio wema kwa vitendo vyao, ujira ambao haukadiriki.

30 Enyi wake wa Nabii! Miongoni mwenu mwenye kufanya makosa yaliyo dhaahiri ubaya wake, basi juu ya adhabu yake zinaongezwa adhabu mbili, ili iwe adhabu tatu kwa kulinganisha na mwenziwe. Na kuongeza huko kwa Mwenyezi Mungu ni kwepesi.

31 Na katika nyinyi mwenye kudumu juu ya kumnyenyekea Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akatenda mema, Mwenyezi Mungu atampa ujira mara mbili. Na tumemuandalia kwa Akhera riziki ya kipimo kizuri.

32 Enyi wake wa Mtume! Nyinyi si kama wanawake wengine kwa fadhila na utukufu. Kama mnataka

33. Na kaeni majumbani kwenu, wala msijishauwe kwa majishauwo ya kijahilia ya kizamani. Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni baarabara.³³

34. Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Mwenyezi Mungu na hikima. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo ya siri, na Mwenye khabari.³⁴

35. Hakika Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, na Waumini wanaume na Waumini wanawake, na wat'iifu wanaume na wat'iifu wanawake, na wasemao kweli wanaume na wanawake, na wanao subiri wanaume na wanawake, na wanyenyekevu wanaume na wanawake, na watoao sadaka wanaume na wanawake, na wanao funga wanaume na wanawake, na wanao jihifadhi tupu zao wanaume na wanawake, na wanao mdhukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wanaume na wanawake, Mwenyezi Mungu amewaandalia msamaha na ujira mkubwa.³⁵

36. Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi.³⁶

37. Na ulipo mwambia yule Mwenyezi Mungu aliye mneemesha, nawe ukamneemesha: Shikamana na mkeo, na mche Mwenyezi Mungu. Na ukaficha nafsini mwako aliyo taka Mwenyezi Mungu kuyafichua, nawe ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye mwenye haki zaidi kumchelea. Basi Zaid alipo kwisha haja naye tulikuoza wewe, ili isiwe taabu kwa Waumini kuwaoa wake wa watoto wao wa kupanga watapo kuwa wamekwisha timiza nao shurutu za t'alaka. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni

uchamngu, basi msizungumze kwa maneno ya kuregeza sauti, hata ambaye ana uharibifu katika moyo wake akaingia tamaa. Kusema kwenu kuwe kama kawaida sio kujitia.

33 Na kaeni nyumbani kwenu, wala msitoke ila kwa haja. Wala msidhihirishe uzuri wenu na mapambo yenu kwa wanaume pale mnapo toka, kama walivyo kuwa wakifanya watu wa ujahili wa zamani. Na timizeni Sala kwa ukamilifu, na toeni Zaka, na fuateni amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hakika Mwenyezi Mungu anataka, kwa yote anayo kuamrisheni na kukukatazeni, mpate utukufu na hishima, ili muondokewe na madhambi na maasia, enyi Ahli Baiti Nnabii, Watu wa Nyumba ya Nabii, na akusafisheni kwa usafi usio kuwa na shaka.

34 Na hifadhini yanayo somwa katika nyumba zenu ya Qur'ani aliyo iteremsha Mwenyezi Mungu, na hikima zililo sawa za Mtume wa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua mambo yalio zama ndani kabisa na ya hakika yake. Basi tahadharini na kwenda kinyume naye na kumuasi Mtume wake.

35 Hakika wenye kut'ii miongoni mwa wanaume na wanawake, na wenye kumsadiki Mwenyezi Mungu na Mtume wanaume na wanawake, na wenye kusimama kwa ut'iifu wanaume na wanawake, na walio wa kweli katika kauli zao na vitendo vyao katika wanaume na wanawake, na wenye kusemba katika kubeba mashaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wanaume na wanawake, na wanyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu wanaume na wanawake, na wenye kuzihifadhi tupu zao kwa yasiyo kuwa halali wanaume na wanawake, na wenye kumdhukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi katika nyoyo zao na ndimi zao wanaume na wanawake, Mwenyezi Mungu amewaandalia kuwasamehe madhambi yao, na kuwalipa malipo makubwa kwa vitendo vyao.

36 Haimjuzii Muumini, mwanamume au mwanamke, kuwa na khiari katika jambo lolote baada ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake wakisha lihukumia. Na mwenye kwenda kinyume na alivyo hukumu Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi amejitenga mbali na njia iliyo sawa kwa umbali ulio dhaahiri.

yenye kutekelezwa.³⁷

38. Hapana ubaya kwa Nabii kufanya aliyo mhalalishia Mwenyezi Mungu. Huo ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu kwa walio pita zamani. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni kudura iliyo kwisha kadiriwa.³⁸

39. (Hao wa zamani) walio kuwa wakifikisha risala za Mwenyezi Mungu na wanamwogopa Yeye, na wala hawamwogopi yeyote isipo kuwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ndiye atoshaye kuhisabu.³⁹

40. Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.⁴⁰

41. Enyi mlio amini! Mdhukuruni Mwenyezi Mungu kwa wingi wa kumdhukuru.⁴¹

42. Na mtakaseni asubuhi na jioni.⁴²

43. Yeye na Malaika wake ndio wanakurehemuni ili kukutoeni gizani mwende kwenye nuru. Naye ni Mwenye kuwarehemu Waumini.⁴³

44. Maamkiano yao siku ya kukutana naye yatakuwa: Salama! Na amewaandalia malipo ya ukarimu.⁴⁴

45. Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekutuma uwe shahidi na mbashiri na mwonyaji,⁴⁵

46. Na mwitaji kumwendea Mwenyezi Mungu kwa idhini yake, na taa yenye kutoa nuru.⁴⁶

37 Na kumbuka pale ulipo mwambia Zaid bin Haritha, ambaye Mwenyezi Mungu amemneemsha kwa kumwongoa kwenye Uislamu, na wewe ukamneemsha kwa kumlea na kumkomboa utumwani: Shikamana na mkeo, Zainab binti Jahsh, na umche Mwenyezi Mungu, na vumilia kukaa naye. Na wewe ulikuwa unaficha nafsi mwako ambayo Mwenyezi Mungu atakuja yadhahirisha, yaani kuwa yeye atampa t'alaka na wewe utakuja muwoa. Nawe ukakhofu watu wasije kukulaumu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anaye stahiki umkhofu, ijapo kuwa hayo ni mashaka juu yako. Basi Zaid alipo kwisha haja naye, na akampa t'alaka kujiondolea dhiki ya kuishi naye, tukakuoza wewe, ili iwe ni chanzo cha kuvunja ada iliyo mbovu. Baada ya hayo hapana ubaya tena kwa Waislamu kuwaoa walio kuwa wake za walio kuwa wamewapanga utoto, baada ya kwisha wat'aliki. Na amri ya Mwenyezi Mungu aitakayo ni lazima iwe bila ya pingamizi.

38 Nabii hana makosa kutenda kitendo alichu muamrisha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ameweka mwendo huo kwa Manabii walio tangulia, kuwa wasipige marfuku alichu wahalalishia na akawakunjulia. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni kupitisha alichu pitisha, na hukumu iliyo thibiti.

39 Manabii hao ndio walio wakifikisha watu ujumbe wa Mwenyezi Mungu kama tulivyo wateremshia. Nao wanamkhofu Yeye, wala hawamkhofu yeyote asiye kuwa Yeye. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Yeye ndiye Muangalizi Mwenye kuhisabu.

40 Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu hata iwe ni haramu kwake kumwoa mt'alaka wake. Lakini yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na ni Mwenye kukhitimisha Manabii wote. Juu yake ni kufikilisha ujumbe kama alivyo muamrisha Mola wake Mlezi, bila ya kumchelea yeyote. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuvizunguka vitu vyote kwa ujuzi wake.

41 Enyi ambao mmeamini! Msifuni Mwenyezi Mungu kwa namna mbali mbali za sifa, na mfanye hayo kwa wingi. Na mtakaseni na kila kisicho kuwa laiki naye mwanzo wa mchana na mwisho wake.

42 Tazama tanbihi ya 41.

43 Na Yeye ndiye aliye kuahidini kukupeni rehema yake na upole wake. Na Malaika wake wanakuombeeni maghfira na uwongofu, ili Mwenyezi Mungu akutoeni kwenye giza la ukafiri na upotovu, mwende kwenye nuru na ut'iifu. Na Mwenyezi Mungu hakika ni Mkuu wa kuwarehemu Waumini.

44 Maamkio yao siku watakapo kutana naye ni: Amani na Salama kwao. Na amewatengezea kwa vitendo vyao ujira wa ukarimu utakao waonyesha fadhila zake.

45 Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekutuma kwa watu wote uwapelekee ujumbe wa Uislamu. Ushuhudie Haki, na uwabashirie Waumini kwamba watapata kheri na thawabu, na uwaonye makafiri kuwa watapata mwisho muovu.

46 Na umetumwa uwe ni mwenye kuwaita viumbe vyote vimwendee Mwenyezi Mungu kwa amri yake.

47. Na wabashirie Waumini ya kwamba wana fadhila kubwa inayo toka kwa Mwenyezi Mungu.⁴⁷
48. Wala usiwat'ii makafiri na wanaafiki, na usijali udhia wao. Nawe mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Mtegemewa.⁴⁸
49. Enyi mlio amini! Mkiwaoa wanawake, Waumini, kisha mkawapa t'alaka kabla ya kuwagusa, basi hamna eda juu yao mtakayo ihisabu. Basi wapeni cha kuwaliwaza, na muwawache kwa kuwachana kwa wema.⁴⁹
50. Ewe Nabii! Tumekuhalalishia wake zako ulio wapa mahari yao, na ulio wamiliki kwa mkono wako wa kulia katika alio kupa Mwenyezi Mungu, na mabinti ami zako, na mabinti wa shangazi zako, na mabinti wa wajomba zako, na mabinti wa dada za mama yako walio hama pamoja nawe; na mwanamke Muumini akijitoa mwenyewe kwa Nabii, kama mwenyewe Nabii akitaka kumwoa. Ni halali kwako wewe tu, si kwa Waumini wengine. Sisi tunajua tuliyo wafaridhia wao katika wake zao na wanawake ilio wamiliki mikono yao ya kulia. Ili isiwe dhiki kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁵⁰
51. Unaweza kuakhirisha zamu kwa umtakaye katika wao, na umsogeze umtakaye. Na kama ukimtaka yule uliye mtenga, basi si vibaya kwako. Kufanya hivi kutapelekea yaburudike macho yao, wala wasihuzunike, na wawe radhi juu ya kile unacho wapa wao wote. Na Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo nyoyoni mwenu, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima.⁵¹
52. Baada ya hawa hawakuhalaliki wewe wanawake wengine, wala kuwabadilisha kwa wake wengine ingawa uzuri wao ukikupendeza; isipo kuwa yule uliye mmiliki kwa mkono wako wa kulia. Na Mwenyezi Mungu anachungua kila kitu.⁵²

Na uwe ni taa ya uwongofu kuwaongoa kwa nuru yake waliopo katika kiza cha shaka.

47 Na wabashirie Waumini kwamba watapata kheri kubwa ya kuzidi katika dunia na Akhera.

48 Na wala usiwafuate makafiri na wanaafiki, wala usijishughulishie na maudhi yao. Na mfanye Mwenyezi Mungu ndiye Wakili wako wa kumtegemea kukulinda na madhara yao na shari zao. Na Mwenyezi Mungu anakutosha kabisa kuwa ndiye Mtegemewa wa kukukifia na kukukinaisha.

49 Enyi mlio amini! Mkifunga ndoa na wanawake Waumini, kisha mkawat'aliki kabla ya hamjawaingilia, basi haiwalazimu eda wao mkawa mnaihisabu. Basi wapeni kitu katika mali kwa kuwapoza. Na mwatote majumbani kwenu bila ya kuwaletea madhara yoyote.

50 Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekuhalalishia wake zako ulio wapa mahari. Na tumekuhalalishia wajakazi ulio wamiliki mkono wako wa kulia, katika alio kuneemeshea Mwenyezi Mungu. Na tumekuhalalishia kuwaoa mabinti ami zako, na mabinti wa shangazi zako, na mabinti wa wajomba zako, na mabinti wa dada, yaani ndugu wa kike, wa mama yako, walio hama nawe. Na tumekuhalalishia mwanamke Muumini akijitolea nafsi yake bila ya mahari, nawe ikawa unataka kumwoa na umempenda. Kujitolea huku ni kwako wewe tu, si kwa Waumini wengine. Kwao haifai hivyo. Tunajua hukumu tulizo wafaridhia Waumini kwa wake zao na wajakazi wao, na tuliyo kuruhusu wewe, si wao, ili isiwe dhiki juu yako kwa tuliyo kuhukumuia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe madhambi ya waja wake, Mwenye kuwarehemu kwa ukunjufu.

51 Unaweza kumuakhirisha umtakaye katika kugawa zamu, na ukamjongeza umtakaye. Na kumtaka uliye muakhirisha zamu yake hapana lawama juu yako. Hivyo kuachiliwa utakavyo wewe yakaribia zaidi kupelekea furaha yao na baada ya kuwahuzunikia, na wao wote wawe radhi kwa ulio wapa. Na Mwenyezi Mungu anayajua yaliomo ndani ya nyoyo zenu, ya kuudhika au kuridhika kwa aliyo kufanyieni sharia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua yaliomo vifuani, Mpole hafanyi papara kuadhibu.

52 Hawakuhalaliki wanawake wengine baada ya hawa, wala kuwapa t'alaka kwa ajili ya kuwabadilisha kwa wengine uwatakao, hata wakikupendeza kwa uzuri wao. Lakini Mwenyezi Mungu amekuhalalishia wajakazi ulio wamiliki kwa mkono wako. Na Mwenyezi Mungu anachungua kila kitu, na anakihifadh.

53. Enyi mlio amini! Msiingie nyumba za Nabii ila mpewe ruhusa kwenda kula, sio kungojea kiwive. Lakini mtakapo itwa basi ingieni, na mkisha kula tawanyikeni, wala msiweke mazungumzo. Hakika hayo yanamuudhi Nabii naye anakustahini, lakini Mwenyezi Mungu hastahi kwa jambo la haki. Na mnapo wauliza wakeze haja waulizeni nyuma ya mapazia. Hivyo ndio usafi zaidi kwa nyoyo zenu na nyoyo zao. Wala haikufalieni kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu, wala kuwaoa wake zake baada yake kabisa. Hakika jambo hilo ni kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.⁵³

54. Mkidhihirisha chochote kile, au mkikificha, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.⁵⁴

55. Hapana ubaya kwao (wake za Mtume) kuonana na baba zao, wala watoto wao, wala ndugu zao, wala watoto wa ndugu zao wanaume, wala watoto wa ndugu zao wanawake, wala wanawake wenzao, wala wale iliyo wamiliki mikono yao ya kulia. Na enyi wanawake, mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushuhudia kila kitu.⁵⁵

56. Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu.⁵⁶

57. Hakika wanao muudhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Mwenyezi Mungu amewalaani duniani na Akhera, na amewaandalia adhabu ya kufedhehi.⁵⁷

58. Na wale wanao waudhi Waumini wanaume na wanawake pasina wao kufanya kosa lolote, bila ya shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zililo dhaahiri.⁵⁸

59. Ewe Nabii! Waambie wake zako, na binti zako, na wake za Waumini wajiteremshie nguo zao. Hivyo ni karibu zaidi kuweza kutambulikana wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁵⁹

53 Enyi mlio amini! Msiingie nyumba za Nabii ila kwa idhini yake kwa ajili ya kwenda kula chakula, bila ya kwenda kungoja wakati mpaka kitapo kuwa tayari. Lakini Mtume akikuiteni, basi ingieni. Na mkisha kula ondokeni. Wala msikae baada yake mkijizoeza mazungumzo nyinyi kwa nyinyi. Kwani hakika kuingia bila ya idhini yake, na kukaa muda mrefu baada ya kwisha kula, kunamuudhi Nabii, naye anakustahini awezi kukutakeni mtoke. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu hana la kumzuia asitangaze haki kama wanavyo zuilikana viumbe. Na mtakapo wauliza wake za Nabii s.a.w. haja yoyote, basi waulizeni nyuma ya mapazia. Hivyo ni usafi bora kwa nyoyo zenu na nyoyo zao zisiingiwe na uchochezi wa Shetani. Na haikufalieni nyinyi kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu, wala kuwaoa wake zake baada yake milele, kwa sababu ya hishima yake na yao. Hakika jambo hilo ni dhambi kubwa kwa Mwenyezi Mungu. (*Tazama Maelezo 33:53*)

54 Mkidhihirisha walau kidogo katika mambo yanayo muudhi, au mkikificha katika vifua vyenu, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.

55 Hapana dhambi kwa wakeze Nabii wakitojificha kwa baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au watoto wa ndugu zao wa kiume, au watoto wa ndugu zao wa kike, au wanawake Waumini wengine, au watumwa walio wamiliki, kwa sababu ya shida ya kuwahitajia kwa matumishi. Nanyi wanawake, mcheni Mwenyezi Mungu katika mambo aliyi kuamrishi, wala msipindukie mipaka yake. Kwani Yeye hakika anajua kila kitu, hapana kilicho fichikana kwake..

56 Hakika Mwenyezi Mungu anamrehemu Nabii wake na yu radhi naye. Na Malaika wanamwombea yeye. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu.

57 Hakika wanao muudhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kuwapinga na kuchochea watu wawakatae, Mwenyezi Mungu amewafukuza kwenye rehema yake duniani na Akhera; na amewaandalia adhabu itayo wavunja kiburi chao.

58 Na wanao waudhi Waumini wanaume na wanawake kwa maneno au vitendo, bila ya wao kufanya makosa yoyote, hao basi wamebeba migongoni mwao mzigo wa ule uwongo wao, na inakuwa wametenda dhambi iliyo dhaahiri ubaya wake.

59 Ewe Nabii! Waambie wake zako, na binti zako, na wake wa Waumini, wateremshe nguo zao juu ya miili

60. Kama wanaafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao, na waenezao fitna katika Madina hawatoacha, basi kwa yakini tutakusalitisha juu yao, kisha hawatakaa humo karibu yako ila muda mchache tu.⁶⁰
61. Wamelaanika! Popote watakapo onekana watakatwa na watauliwa kabisa.⁶¹
62. Hii ni ada ya Mwenyezi Mungu iliyo kuwa kwa wale walio pita zamani. Wala hutapata mabadiliko katika ada ya Mwenyezi Mungu.⁶²
63. Watu wanakuuliza khabari ya Saa (ya Kiyama). Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Na nini kitakujuyva? Pengine hiyo Saa iko karibu.⁶³
64. Hakika Mwenyezi Mungu amewalaani makafiri na amewaandalia Moto unao waka kwa nguvu.⁶⁴
65. Watadumu humo milele. Hawampati mlinzi wala wa kuwanusuru.⁶⁵
66. Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa katika Moto. Watasema: Laiti tungeli mt'ii Mwenyezi Mungu, na tungeli mt'ii Mtume!⁶⁶
67. Na watasema: Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwat'ii bwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio walio tupoteza njia.⁶⁷
68. Mola wetu Mlezi! Wape wao adhabu mara mbili, na uwalaani laana kubwa.⁶⁸
69. Enyi mlio amini! Msiwe kama wale walio mtaabisha Musa, lakini Mwenyezi Mungu akamtakasa na waliyo yasema, naye alikuwa mwenye hishima mbele ya Mwenyezi Mungu.⁶⁹
70. Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya sawasawa.⁷⁰
71. Apate kukutengenezeni vitendo vyenu na akusameheni madhambi yenu. Na anaye mt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio

yao. Na wakivaa namna hii ni afadhali na wanaelekea zaidi kijuulikana na kwa hivyo wasipate kuudhiwa. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye kumrehemu mwenye kuacha madhambi yake.

60 Ninaapa! Ikiwa hawataacha hao wanaafiki, na wenye maradhi katika nyoyo zao, na wanao eneza khabari za uwongo katika Madina, hapana shaka nitakusalitisha juu yao, kisha hawatabakia kuwa karibu yako ila kwa muda mchache tu.

61 Hao wanastahiki laana na kufukuzwa. Kila watapo patikana wakamatwe na wauliwe moja kwa moja. 62 Mwendu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu tangu zamani, kwa walio kuwa wakiwafanyia unaafiki Manabii na Mitume, na wakiasi, ni kuwa huuwawa kila wanapo kutikana. Wala mwendo wa Mwenyezi Mungu haugauki.

63 Watu wanakuuliza lini itasimama Saa ya Kiyama. Waambie hao: Hakika ujuzi wa wakati wake uko kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Na nini kitakujuyva? Pengine wakati wa kusimama Saa ya kiyama upo karibu.

64 Hakika Mwenyezi Mungu amewafukuza makafiri kwenye rehema yake, na amewatengenezea Moto mkali mno.

65 Hawatatoka humo kabisa. Hawatampata wa kuchukua dhamana ya kuwahami, wala wa kuwatetea.

66 Siku zitakapo geuka nyuso zao Motoni kutoka hali hii kwendea hali hiyo, wakisema kwa majuto: Laiti kuwa sisi tulim'ii Mwenyezi Mungu na tungeli mt'ii Mtume!

67 Na watasema: Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwafuata maraisi wetu, na wakubwa wetu katika kukukataa Wewe na Mtume wako. Na wao ndio wakatutenganisha mbali na Njia Iliyo Nyooka.

68 Mola wetu Mlezi! Wajaalie adhabu yao iwe mardufu, na uwafukuze kwenye rehema yako kabisa kwa kadri ya madhambi yao na makosa yao.

69 Enyi mlio amini! Msimuudhi Nabii kwa namna yoyote ya udhia, kama wale walio muudhi Musa katika kaumu yake. Na Mwenyezi Mungu akamtoa makosani na akamsafisha na hayo waliyo mzulia. Na Musa mbele ya Mwenyezi Mungu alikuwa ni bwana mwenye hadhi.

70 Enyi mlio amini! Iogopeni adhabu ya Mwenyezi Mungu mkimuasi, na semeni maneno yalio simama sawa yasio kwenda upogo.

makubwa.⁷¹

72. Kwa hakika Sisi tulikadimisha amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhaalimu mjinga.⁷²

73. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu anawaadhibu wanaafiki wanaume, na wanaafiki wanawake, na washirikina wanaume, na washirikina wanawake; na anawapokelea toba Waumini wanaume, na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁷³

71 Apate kukuwezesheni kutenda mema, na azifute dhambi zenu. Na mwenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi huyo amepata kufuzu kukubwa kwa kuepuka adhabu, na kupata thawabu.

72 Sisi kwa hakika tulizitaka mbingu na ardhi na milima zichukue dhamana, nazo zikakataa kuichukua, na wakaiogopa. Lakini mwanaadamu aliichukua. Hakika yeye amekuwa ni mkubwa wa kujidhulumu nafsi yake kwa kutojua jukumu la kuchukua huko.

73 Ili Mwenyezi Mungu awaadhibu wanaafiki wanaume, na wanaafiki wanawake, na washirikina wanaume, na washirikina wanawake; na Mwenyezi Mungu apate kukubali toba za Waumini wanaume, na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghira, Mwingi wa rehema.

Sura 34 - Saba'

Utangulizi

Sura hii imeanzia kwa kumfanya Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kustahiki kusifiwa na kuhimidiwa kwa alivyo waneemesha waja wake. Kwani vyote vilioko mbinguni na katika ardhi ni vyake Yeye kwa kuviumba na kuvimiliki. Na Sura inaeleza porojo la makafiri juu ya Saa ya Kiyama, na kukanya kwao kufufuliwa, na kumsingizia Mtume kuwa ni mwongo na mwendawazimu. Na Mwenyezi Mungu *Subhanahu* anawarejesha kwenye dalili za uweza wake, na anawahadharisha kuwa atawateremshia kama alivyo wateremshia walio kama wao, ikawameza ardhi, au vikawaangukia vipande kutoka mbinguni. Na anawakumbusha anavyo wafanyia vipenzi vyake. Kama alivyo mlainishia chuma Daudi, na akamtawalisha Sulaiman na akawafanya majini wantumikie, wakafanya kama alivyo taka, kama mihrabu na masanamu. Na Daudi na Suleiman waliishukuru neema, na wachache tu katika waja wa Mwenyezi Mungu wanao shukuru. Hayo yakafuatia maelezo ya neema aliyo waneemesha Mwenyezi Mungu watu wa Sabaa, nao wasishukuru. Hao walikuwa na bustani mbili, ya kulia na kushoto. Miji yao ilikuwa imekaribiana, na wakisafiri baina yao kwa amani. Neema ikawatia kiburi, wakataka safari ziwe ndefu zaidi. Mwenyezi Mungu akawalipa anavyo walipa wanao zikataa neema zake. Nao wakatimiza aliyo fikiri Iblisi na wakamfuata. Na yeye hakuwa na madaraka juu yao, lakini hayo yalikuwa ni mtihani tu wapate kutengana baina ya wanao iamini Akhera na wenye shaka nayo. Kisha Sura ikaingia kuwaeleza hao wanao wafanya kuwa ni miungu kwamba kwa hakika hawana lolote wawezalo. Na inakumbusha Sura kuwa kila mtu ana jukumu la makosa ayatendayo. Na ikathibitisha Ujumbe wote wa Mtume. Na ikataja kuwa washirikina wanaiona Siku ya Kiyama inachelewa. Na hiyo ina wakati wake maalumu.

Na Sura inasimulia kauli ya makafiri katika Qur'ani, na majadiliano baina ya wakuu na wanyonge, na ikaweka mipaka ya kujifakhari kwa mali na wana, na kwamba hayo mali hayamkaribishi mtu kwa Mwenyezi Mungu ila kwa kadri ya manufaa kwa watu yanayo patikana kutokana na mali hayo. Kwani hayo mali ni milki yake Mwenyezi Mungu. Na Yeye humkunjulia riziki amtakaye na humdhikisha. Na inawekwa wazi sura ya washirikina. Kwani wao walimwambia Mtume wao kwamba yeye anataka kuwazuilia wasiabudu miungu walio kuwa wakiiabudu baba zao. Na wakaisema Qur'ani aliyo teremshiwa kuwa ni uzushi ulio tungwa, na uchawi dhaahiri! Na pia walidai kuwa hawakupewa Vitabu kabla yake, wala hakutumwa Mtume kabla yake. Na hali hakika tuliwatumia walio kabla yao wanao wajua nguvu zao, na utukufu wao, na khabari zao. Na walipo kuwa hawakuitikia Wito tuliwashika kwa kuwaadhibu. Na Mtume s.a.w. anaamrisha aeleze wazi ujumbe wake muhimu kwao. Na hili ni kumbusho bila ya kahari. Na wanaamrisha wantazame huyu mwenzao. Hana wazimu, wala hataki mali, na Wito wake kwa watu wafuate Haki ni kwa Ufunuo (Wahyi) unao tokana na Mwenyezi Mungu Mtukufu ili wapate amani. Na itakapo kuja Saa ya Kiyama watafazaika, na watakuwa hawana pa kukimbilia, na watakatwa pahala karibu. Hapo tena ndio watasema: Tumeamini! Yafaa nini tena hapo Imani nao walikwisha kataa kabla yake. Watazuiwa baina yao na wanacho kitamani, kama walivyo fanyiwa walio kuwa mfano wao. Wao wote walikuwa na shaka tupu katika mambo ya Dini.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, ambaye ni vyake vyote viliomo mbinguni na katika ardhi. Na sifa ni zake Yeye katika Akhera. Naye ni Mwenye hikima, Mwenye khabari.¹
2. Anajua yanayo ingia katika ardhi na yanayo toka humo, na yanayo teremka kutoka mbinguni, na yanayo panda huko. Na Yeye ni Mwenye kurehemu, Mwenye kusamehe.²
3. Na walisema walio kufuru: Haitatufikia Saa (ya Kiyama). Sema: Kwani? Hapana shaka itakufikieni, naapa kwa haki ya Mola wangu Mlezi, Mwenye kujua ya ghaibu! Hapana kinacho fichikana kwake hata chenye uzito wa chembe tu, si katika mbingu wala katika ardhi, wala kilicho kidogo kuliko hivyo, wala kikubwa zaidi; ila vyote hivyo vimo katika Kitabu chake chenye kubainisha.³
4. Ili awalipe walio amini na wakatenda mema. Hao watapata msamaha na riziki ya ukarimu.⁴
5. Na wale walio jitahidi kuzipinga Ishara zetu wakaona watashinda, hao watapata adhabu mbaya yenye uchungu.⁵
6. Na walio pewa ilimu wanaona ya kuwa ulio teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi ni haki, nayo huongoa kwendea njia ya Mwenye nguvu, Mwenye kusifiwa.⁶
7. Na walio kufuru walisema: Je! Tukujuulisheni mtu anaye kuambieni kwamba mtakapo Chambuliwa mapande mapande mtakuwa katika umbo jipya?⁷
8. Ama amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, au ana wazimu. Bali wasio amini

1 Sifa zote nzuri ni haki ya Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye Mwenye kuumba, na Mwenye kumiliki, na Mwenye kupanga vyote vilioko mbinguni, na vilioko katika ardhi. Na Yeye peke yake ndiye Mwenye sifa Akhera, kwa kutamalaki kwake kuliko enea. Naye ndiye Mwenye hikima asiye kosa, Mwenye khabari zote, hapana asicho kijua siri yake.

2 Anajua kila kinacho ingia katika sehemu za ardhi, kama maji, na khazina, na vilio zikwa, na sehemu za maiti; na kila kinacho toka, kama wanyama, na mimea, na maadeni, na maji ya visima, na chemchem. Na anajua vinavyo teremka kutoka mbinguni, kama Malaika, na Vitabu wanavyo vipokea Manabii, na mvua, na radi; na anajua vinavyo panda ndani yake na kwendea huko, kama Malaika, na a'mali za ibada, na roho. Na Yeye ni Mwingi wa rehema, Mkubwa wa kusamehe.

3 Na wenye kukufuru wakasema: Haitujii Saa iliyo ahidiwa kuwa ni ya kufufuliwa na kukusanywa watu. Waambie ewe Mtume! Hapana shaka itakujieni, nami naapa kwa Mola wangu Mlezi, Mwenye kujua ya siri, ambaye hapana chenye kughibu na ujuzi wake hata ingawa kiasi ya chembe tu, si katika mbingu wala katika ardhi. Wala kilicho kidogo kuliko chembe, wala kikubwa kuliko hivyo hakikosi kuandikwa katika Kitabu kilicho timia, chenye kubainisha kila kitu. (*Tazama Maelezo 34:3*)

4 Ili Mwenyezi Mungu awathibitisha walio amini na wakatenda mema kwa ajili ya nafsi zao na kwa ajili ya watu wengine. Hao Waumini watendaji watapata kwa Mwenyezi Mungu msamaha wa kuwafutia madhambi yao, na riziki kunjufu isiyo na masimbulizi ndani yake.

5 Na hao walio zishughulisha nafsi zao kuipiga vita Qur'ani kutaka kuishinda amri ya Mwenyezi Mungu katika kumsaidia Mtume wake, hao watapata adhabu katika adhabu za mwisho wa ubaya na uchungu.

6 Na walio neemeshwa na Mwenyezi Mungu kwa kupewa ujuzi kuwa Qur'ani ulio teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi, yenye ndani yake mambo ya itikadi na uwongofu, ni Haki isiyo kuwa na shaka yoyote, wanajua kuwa hiyo ndiyo yenye kuwaongoa watu kwendea Njia ya Mwenyezi Mungu, Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye kustahiki kila sifa njema.

7 Na makafiri waliambiana wenyewe kwa wenyewe, kwa kufanyia kejeli kufufuliwa: Je! Tukuonyesheni mtu ataye kuambieni kwamba mtapo kwisha kufa, na viwiliwili vyenu vikagawika mapande mapande kuwa ati mtafufuliwa tena kwa umbo jipya?

Akhera wamo adhabuni na upotofu wa mbali kabisa.⁸

9. Kwani hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao ya mbingu na ardhi? Tungeli penda tungeli wadidimiza ndani ya ardhi, au tungeli wateremshia juu yao vipande vya mbingu. Hakika katika haya zipo Ishara kwa kila mja aliye tubia.⁹

10. Na tulimpa Daudi fadhila kutoka kwetu, (tukasema): Enyi milima! Karirini kumtakasa Mwenyezi Mungu pamoja naye! Na ndege pia. Na tukamlainishia chuma.¹⁰

11. (Tukamwambia:) Tengeneza nguo za chuma pana, na kadiria sawa katika kuunganisha. Na tendeni mema. Hakika Mimi nayaona vyema mnayo yatenda.¹¹

12. Na Suleiman tuliufanya upepo umtumikie. Safari yake ya asubuhi ni mwendo wa mwezi mmoja, na safari yake ya jioni ni mwendo wa mwezi mmoja. Na tukamyayushia chemchem ya shaba. Na katika majini walikuwako walio kuwa wakifanya kazi mbele yake kwa idhini ya Mola wake Mlezi. Na kila anaye jitenga na amri yetu katika wao, tunamwonjesha adhabu ya Moto unao waka.¹²

13. Walikuwa wakimfanyia alipendalo, kama mihrabu, na masanamu, na madeste makubwa kama mahodhi, na masufuria makubwa yasiyo ondolewa mahala pake. Enyi watu wa Daudi! Fanyeni kazi kwa kushukuru. Ni wachache katika waja wangu wanao shukuru.¹³

14. Na tulipo mhukumia kufa, hapana aliye wajuulisha kufa kwake ila mnyama wa ardhi aliye kula fimbo yake. Na alipo anguka majini walitambua lau kuwa wangeli jua ya ghaibu wasingeli kaa katika adhabu hiyo ya kufedhehesha.¹⁴

15. Hakika ilikuwapo Ishara kwa (watu wa nchi ya) Saba katika maskani yao - bustani

8 Mtu huyu amenzulia uwongo Mwenyezi Mungu kwa kumnasibishia kuwa atawafufua wafu, au mtu huyu ana wazimu ndio anasema asiyo yajua? Siyo hayo wayasemayo. Bali ukweli wa mambo ni kuwa hao wasio iamini Akhera wataingia katika adhabu na upotovu wa kupotelea mbali na Haki.

9 Je! Wamepofuka, hata hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao ya mbinguni na katika ardhi wakaujua uweza wetu wa kutenda tuyatakayo? Tukitaka ardhi iwameze, tutawazamisha. Au tungeli taka viwaangukie vipande vya mbingu tuwasage sage tungeli wateremshia. Hakika katika tuliyo yataja zipo dalili kwa kila mja mwenye kurejea kwa Mola wake Mlezi katika kila jambo lake.

10 Wallahi! Kwa hakika tulimpa Daudi fadhila kutoka kwetu kwa kumpa hikima na Kitabu. Na tulisema: Enyi milima! Karirini pamoja naye Tasbihi kumtakasa Mwenyezi Mungu, pale anapo sabihi yeye. Na Sisi tuliwafanya ndege pia wamtumikie, nao wawe wakikariri kumtakasa Mwenyezi Mungu. Na tukakifanya chuma kiwe laini kwake aunde kwa sura atakayo. (*Tazama Maelezo 34:10*)

11 Tulimfunulia kumwambia aunde nguo za chuma pana za kujilinda katika vita na maadui. Naye azifume kwa hikima na ustadi katika kuviunga viungo vyake. Na tukamwambia yeye na watu wake: Tendeni yatakayo kuleteeni kheri na maslaha. Hakika Mimi nayaona vyema yote myatendayo, hapana kinacho niporonyoka nisikione.

12 Na Suleiman tukamfanyia upepo umtumikie. Mwendo wake wakati wa asubuhi mmoja ni sawa na safari ya dasturi inayo chukua mwezi mzima. Na mwendo wake wakati wa jioni moja ni kama safari ya kuchukua mwezi. Na tukamyayushia maadeni ya shaba ikawa inatiririka kwa wingi moja kwa moja. Na tukawafanya majini wawe wakimtumikia mbele yake kwa amri ya Mola wake Mlezi. Na yeyote katika majini aliye wacha kut'ii amri ya Suleiman basi tulimwonjesha adhabu ya Moto unao waka kwa nguvu.

13 Hao majini wakifanya atakacho Suleiman, kama misikiti kwa ajili ya ibada, na masanamu, na madeste au mabakuli makubwa kama mahodhi ya maji, na vyombo vya kupikia, yaani masufuria, makubwa yaliyo kaa pale pale penye mafya yake hayaondoki kwa kuwa ni makubwa mno. Na tukawaambia watu wa Daudi: Tendeni kazi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu vilivyo. Na ni wachache miongoni mwa waja wangu ambao wanakumbuka neema zangu wakawa wananishukuru kwa wingi.

14 Tulipo mhukumia Suleiman mauti, hapana aliye waonyesha majini kuwa kesha kufa ila kinyama cha ardhi kilicho ila fimbo yake aliyo kuwa akiiegemea. Alipo anguka majini wakajua kuwa lau kuwa wangeli jua ya ghaibu wasingeli endelea na ile adhabu ya mashaka ya kuwadhalilisha.

mbili, kulia na kushoto. Kuleni katika riziki ya Mwenyezi Mungu, na mumshukuru. Mji mzuri na Mola Mlezi aliye Msamehevu.¹⁵

16. Lakini wakaacha. Tukawapelekea mafuriko makubwa, na tukawabadilishia badala ya bustani zao hizo kwa bustani nyengine zenye matunda makali machungu, na mivinje, na kidogo katika miti ya kunazi.¹⁶

17. Hayo tuliwalipa kwa sababu ya walivyo kufuru. Nasi kwani tunamuadhibu isipo kuwa anaye kufuru?¹⁷

18. Na baina yao na miji mingine tuliyo ibariki tuliweka miji iliyo dhaahiri, na tukaweka humo vituo vya safari. Tukawaambia: Nendeni humo usiku na mchana kwa amani.¹⁸

19. Lakini wakasema: Mola wetu Mlezi! Weka mwendo mrefu baina ya safari zetu. Na wakazidhulumu nafsi zao. Basi tukawafanya ni masimulizi tu, na tukawatawanya tawanya. Hakika katika hayo bila ya shaka zimo Ishara kwa kila mwenye kusubiri sana na akashukuru.¹⁹

20. Na bila ya shaka Iblisi alihakikisha ile dhana yake juu yao. Nao walimfuata, isipo kuwa kundi la Waumini.²⁰

21. Na yeye hakuwa na mamlaka yoyote juu yao, ila kwa sababu ya kuwajaribu tujue nani mwenye kuamini Akhera, na nani anaye tilia shaka. Na Mola wako Mlezi ni Mwenye kuhifadhi kila kitu.²¹

22. Sema: Waite mnao wadaia kuwa ni badala ya Mwenyezi Mungu. Hawamiliki hata uzito wa chembe hichi katika mbingu wala ardhi. Wala hawana ushirika wowote humo. Wala Yeye hana msaidizi miongoni mwao.²²

15 Ninaapa: Hakika katika watu wa Sabaa katika makaazi yao ya Yaman palikuwa na Ishara ya uweza wetu. Zilikuwako bustani mbili zilizo zunguka nchi yao, kulia na kushoto. Wakaambiwa: Kuleni katika riziki ya Mola wenu Mlezi, na mshukuru neema zake kwa kuzitumilia inavyo faa. Huu mji wenu ni mji mzuri, una vivuli na matunda. Na Mola wenu Mlezi ni Mwingi wa maghfira kwa anaye mshukuru.

16 Lakini wao waliacha kushukuru neema, na wakawa maisha yao ya kiburi. Tukawafungulia mafuriko ya nguvu yaliyo tokea baada ya kupasuka kuta za mahodhi, yakateketeza mabustani yao. Tukawabadilishia badala ya bustani zao mbili zile zenye matunda mazuri, zikawa nyengine mbili zenye matunda machungu, na miti isiyo kuwa na matunda, na mikunazi kidogo isiyo toa hamu. (*Tazama Maelezo 34:16*)

17 Hayo ndiyo malipo tuliyo walipa kwa kufuru zao kuzikufuru neema na kuto zishukuru. Na kwani Sisi tunamuadhibu kwa adhabu hii kali yeyote yule ila aliye kuwa mwingi wa kumkufuru Mwenyezi Mungu na fadhila zake?

18 Na tulifanya baina ya maskani yao ya Yaman na baina ya miji mingine iliyo barikiwa miji mingineyo pia iliyo karibiana inaonana. Na tukafanya makhusiano baina yao ni kiasi maalumu cha mwendo usio kuwa wa taabu. Na tukawaambia: Nendeni humo usiku na mchana nanyi mko katika amani.

19 Kwa kutakabari kwa neema, na raha, na amani, walisema: Tuwekee mbali masafa ya safari zetu, tuisadifu kukuta miji iliyo amirishwa ya katikati mpaka tufike huko twendako! Mwenyezi Mungu akazifanya ziwe mbali hizo safari zao. Na wakawa wao wamejidhulumu nafsi zao kwa uasi wao. Tukawafanya hao ni masimulizi ya watu, na tukawatenganisha mtengano mkubwa. Hakika katika yaliyo wapata hao yapo mawaidha kwa kila mwenye kusubiri kwa bala, mwenye kushukuru kwa apewacho.

20 Na bila ya shaka Iblisi amehakikisha dhana yake juu yao. Nao wakamfuata yeye isipo kuwa wachache miongoni mwa Waumini.

21 Na wala Iblisi hakuwa na nguvu za kuwafanya wamt'ii na kumnyenyekea; lakini Mwenyezi Mungu kawafanyia mtihani apate kuwadhihirisha wepi wanao isadiki Akhera, na wepi wana shaka nayo. Ewe Nabii! Mola wako Mlezi ni Mwenye kuchungua kila kitu, Mwenye kusimamia kila kitu.

22 Ewe Nabii! Waambie washirikina: Waombeni hao mnao dai kwa uwongo kwamba ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, wakuleteeni manufaa au wakuondoleeni madhara. Hawakujibuni kitu. Kwani hao hawamiliki hata kiasi ya chembe ya kitu katika mbingu wala katika ardhi. Wala wao hawana ushirika wowote na Mwenyezi Mungu katika kuumba au kumiliki. Wala hapana yeyote katika hao miungu ya

23. Wala uombezi mbele yake hautafaa kitu, isipo kuwa kwa aliye mpa idhini. Hata itapo ondolewa khofu kwenye nyoyo zao watasema: Mola wenu Mlezi kasema nini? Watasema: Yaliyo kweli! Na Yeye ndiye Aliye juu, Mkubwa.²³
24. Sema: Ni nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Sema: Mwenyezi Mungu! Na hakika sisi au nyinyi bila ya shaka tuko kwenye uwongofu au upotofu ulio wazi.²⁴
25. Sema: Nyinyi hamtaulizwa kwa makosa tuliyo yafanya, wala sisi hatutaulizwa kwa mnayo yatenda nyinyi.²⁵
26. Sema: Mola wetu Mlezi atatukusanya, kisha atatuhukumu kwa haki; na Yeye ndiye Hakimu Mwenye kujua.²⁶
27. Sema: Nionyesheni mlio waunganisha naye kuwa washirika. Hasha! Bali Yeye ndiye Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu, Mwenye hikima.²⁷
28. Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui.²⁸
29. Na wanasema: Ahadi hii itakuwa lini, ikiwa nyinyi mnasema kweli?²⁹
30. Sema: Nyinyi mnayo miadi ya Siku ambayo hamtaakhirika nayo kwa saa moja, wala hamtaingulia.³⁰
31. Na walisema walio kufuru: Hatutaiamini Qur'ani hii, wala yaliyo kuwa kabla yake. Na angeli waona madhaalimu watapo simamishwa mbele ya Mola wao Mlezi, wakirudishiana maneno wao kwa wao! Wanyonge wakiwaambia walio takabari: Lau

uwongo anaye msaidia Mwenyezi Mungu katika kupanga mambo ya viumbe vyake.

23 Wala maombezi kwa Mwenyezi Mungu hayawafai ila wenye kustahili makamo ya kuombewa. Mpaka itapo ondoka khofu katika nyoyo zao kwa kutolewa ruhusa ya kuombewa, hapo watakuwa wakiambiana kwa furaha: Mola wenu Mlezi kakwambieni nini? Na wengine watajibu kwamba alilo sema ni kauli ya haki, kwa kutoa ruhusa kuombewa aliye mridhi. Na Yeye peke yake, ndiye Mwenye Utukufu na Ukubwa. Na Yeye ndiye anaye ruhusu na kumkatalia amtakaye.

24 Ewe Nabii! Waambie washirikina: Nani anaye kuleteeni riziki kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Watapo kuwa hawajibu kwa inda tu, waambie: Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anaye kuruzukuni kutoka kote kuwili. Je! Ni sisi Waumini au nyinyi washirikina ndio walio katika moja ya hali mbili, ya uwongofu au upotofu ulio wazi?

25 Ewe Nabii! Waambie: Nyinyi hamuulizwi khabari ya madhambi tuliyo yafanya sisi; wala sisi hatuulizwi khabari ya vitendo vyenu.

26 Waambie: Mola wetu Mlezi atatukusanya Siku ya Kiyama, kisha atatuhukumu kwa haki. Na Yeye *Subhanahu* ndiye Hakimu wa kila shauri, Mwenye kujua kwa hakika yetu sisi na yenu nyinyi.

27 Waambie: Nionyesheni hao mlio waunganisha na Mwenyezi Mungu kwa kustahiki kuabudiwa, mnao dai kuwa ni miungu wa shirika na Yeye. Yeye hana mshirika, bali Yeye ndiye Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye hikima katika kupanga kwake na kuendesha kwake.

28 Na Sisi hatukukutuma ewe Muhammad, ila kwa watu wote. Uwe ni mwenye kuwabashiria Waumini kuwa watapata kheri, na mwenye kuwaonya makafiri kuwa watapata shari. Lakini aghlabu ya watu hawajui ukweli wako, wala kuwa Utume wako ni wa kwa watu wote. (Haya ni kwa sababu hapana Mtume aliye kuja kwa watu wote ila huyu Nabii Muhammad s.a.w. Nabii Musa alikuja kwa Wana wa Israili kuwatoa Misri. Nabii Isa, Yesu Kristo, pia kaja kwa Wana wa Israili tu, kama isemavyo Qur'ani 3.49, na Injili ya Mathayo 10.5-6 Yesu alipo sema: "Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." Na 15.24 alipo sema: "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." Na Injili ya Yohana 17.9)

29 Na makafiri wanasema kwa kuifanya haiwi hiyo Siku iliyo ahidiwa kwa ajili ya malipo: Lini itakuwa ahadi hii tuingie Motoni, na nyinyi muingie Peponi, kama nyinyi ni wakweli kwa hiyo ahadi yenu.

30 Ewe Nabii! Waambie: Miadi yenu ni Siku kubwa mno; ikifika hamto chelewa hata kwa saa moja, wala hamto tangulia.

kuwa si nyinyi, bila ya shaka tungeli kuwa Waumini sisi.³¹

32. Walio takabari watawaambia wanyonge: Kwani sisi ndio tulio kuzuieni na uwongofu baada ya kukujieni? Bali nyinyi wenyewe ni wakosefu.³²

33. Na wanyonge wakawaambia walio takabari: Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipo kuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie washirika. Nao wataficha majuto watakapo iona adhabu. Na tutaweka makongwa shingoni mwao walio kufuru. Kwani wanalipwa ila kwa waliyo kuwa wakiyatenda?³³

34. Na hatukumtuma mwonyaji yeyote kwenye mji, ila walisema walio jidekeza kwa starehe zao wa mji huo: Hakika sisi tunayakataa hayo mliyo tumwa nayo.³⁴

35. Na wakasema: Sisi tuna mali mengi zaidi na watoto, wala sisi hatutaadhibiwa.³⁵

36. Sema: Hakika Mola wangu Mlezi humkunjulia riziki na humdhikisha amtakaye. Lakini watu wengi hawajui.³⁶

37. Na si mali yenu wala watoto wenu watakao kukaribisheni kwetu muwe karibu, isipo kuwa aliye amini na akatenda mema. Hao basi watapata malipo mardufu kwa walio yafanya. Nao watakuwa salama katika maghorofa.³⁷

38. Na wanao jitahidi kuzipinga Ishara zetu, wakaona watahinda, hao watahudhurishwa kwenye adhabu.³⁸

39. Sema: Kwa hakika Mola wangu Mlezi humkunjulia riziki na humdhikisha amtakaye katika waja wake. Na chochote mtakacho kitoa Yeye atakilipa. Naye ni Mbora wa wanao ruzuku.³⁹

31 Na walio kufuru wanasema: Hatuisadiki Qur'ani hii wala hivyo Vitabu vilivyo tangulia kabla yake kwa hayo vinavyo amrisha na kulingania. Na lau ungesi ona - ewe mwenye kuweza kuona - wakati wanapo simamishwa madhaalimu mbele ya Muumba wao, Mwenye kumiliki amri yao, ungeliona maajabu katika msimamo wao, pale wanapo jibizana maneno wao kwa wao. Walio wanyonge wakiwaambia walio tukua juu yao: Ingeli kuwa si nyinyi, kwa kutusaliti na kutamalaki, hapana shaka tungeli kuwa Waumini.

32 Walio takabari na wakajiona ni wakubwa, watawaambia wanyonge, kwa kuyapinga maneno yao: Kwani sisi tulikuzuieni msiongoke ulipo kufikieni uwongofu? Tumekuzuieni sisi au nyinyi wenyewe ndio mmekhiari upotofu kuliko uwongofu.

33 Na wanyonge nao watawaambia walio takabari: Bali vitimbi vyenu na uchochezi wenu kutuchochea usiku na mchana ndio umetutumbukiza katika hilaki, pale mlipo kuwa mkitutaka tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie miungu mingine ya kumshirikisha. Na pande zote mbili zikaficha majuto yao walipo iona adhabu inawashukia. Wakajua kuwa hapana faida ya kuonyesha majuto. Na tukayaweka makongwa, (nira), juu ya shingo za wasio amini. Je! Watu hawa wanastahiki chochote ila malipo kwa yale waliyo kuwa wakiyatenda.

34 Na sisi hatukumtuma Mtume yeyote kwenda kwenye mji kuwaita watu wake wafuate Haki ila wale wanao jidekeza kwa starehe zao katika ule mji husema: Hakika sisi tunayakanusha hayo mliyo kuja nayo.

35 Na husema kwa kujipa: Sisi tuna mali mengi zaidi na watoto. Wala hatutaadhibiwa Akhera.

36 Ewe Nabii! Waambie: Hakika aliye niumba humkunjulia riziki amtakaye, katika wanao muasi na wanao mt'ii. Na humdhikisha amtakaye. Wala hiyo si dalili ya kuwa Yeye yuradhi na mtu au anamchukia. Lakini watu wengi hawajui haya.

37 Wala mali yenu wala watoto wenu sio jambo la kukurubisheni kwetu mkawa karibu. Lakini ambaye Imani yake imethibiti, na akawa anatenda mema, basi watu kama hao ndio watapata thawabu mara mbili kwa waliyo yatenda. Na Peponi watakuwa ni watu wa juu na wenye amani.

38 Na hao ambao wana fanya juhudi kuzipinga Ishara zetu, wakifanya kila hila kuzivunja na kuwazuia Manabii wetu wasifikishe Ujumbe wake, hao, basi watakuwa katika adhabu, wamehudhurishwa na wala hawataepuka.

39 Ewe Nabii! Sema: Hakika Mola wangu Mlezi anamkunjulia riziki amtakaye katika waja wake, na humdhikisha amtakaye. Na chochote mtacho kitoa Yeye atakilipa. Na Yeye Aliye takasika ni Mbora wa wenyewe kuruzuku.

40. Na siku atakayo wakusanya wote, kisha atawaambia Malaika: Je! Hawa walikuwa wakikuabuduni?⁴⁰
41. Waseme: *Subhanak*, Umetakasika. Wewe ndiye kipenzi chetu si hao. Bali wao walikuwa wakiwaabudu majini; wengi wao wakiwaamini hao.⁴¹
42. Hii leo hataweza yeyote kumletea nafuu wala madhara mwenzie. Na tutawaambia walio dhulumu: Onjeni adhabu ya Moto mlio kuwa mkiukanusha.⁴²
43. Na wanapo somewa Aya zetu zilizo wazi wanasema: Huyu si chochote ila ni mtu anaye taka kukuzuieni na waliyo kuwa wakiabudu baba zenu. Na wakasema: Haya si chochote ila ni uwongo ulio zuliwa. Na walio kufuru waliiambia Haki ilipo wajia: Haya si chochote ila ni uchawi ulio dhaahiri.⁴³
44. Wala hatukuwapa Vitabu wavisome, wala hatukuwatumia Mwonyaji kabla yako wewe.⁴⁴
45. Na walikadhibisha walio kuwa kabla yao. Na hawakufikilia hata sehemu moja katika kumi ya tulivyo wapa hao. Nao waliwakadhibisha Mitume wangu. Basi kuangamiza kwangu kulikuwa namna gani!⁴⁵
46. Sema: Mimi nakunasihini kwa jambo moja tu - ya kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili-wawili na mmoja-mmoja; kisha mfikiri. Mwenzenu huyu hana wazimu. Yeye si chochote ila ni Mwonyaji kwenu kabla ya kufika adhabu kali.⁴⁶
47. Sema: Ujira nilio kuombeni ni wenu nyinyi. Sina ujira ila kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye ni Shahidi juu ya kila kitu.⁴⁷
48. Sema: Hakika Mola wangu Mlezi anaondoa upotovu kwa Haki. Yeye ndiye

40 Na taja, ewe Nabii, siku Mwenyezi Mungu atapo wakusanya wote, na kisha *Subhanahu* awaambia Malaika mbele ya wale walio kuwa wakiwaabudu: Je! Hawa walikuabuduni nyinyi khasa badala yangu mimi?

41 Malaika watasema: Sisi tunakutakasa kabisa na kuwa Wewe una mshirika wowote. Wewe ndiye tulio shikamana nawe kwa mapenzi na ut'iifu, sio wao. Hao wameghurika katika madai yao kuwa wanatuabudu sisi. Bali walikuwa wanafuata nyayo za mashetani walio wapambia ushirikina. Wengi wao wakiwasadiki hao.

42 Basi Siku ya Mkusanyo hapana atakaye weza kumletea mwenzie manufaa wala kumkinga na madhara. Na tutawaambia walio jidhulumu nafsi zao: Ionjeni adhabu ya Moto ambayo mlio kuwa duniani mkiikanusha.

43 Na makafiri walipo somewa Aya zetu zilizo wazi dalili zake kuonyesha Haki, makafiri walisema: Huyu si chochote ila ni mtu anaye taka kukuzuilieni msiwaabudu walio kuwa wakiwaabudu baba zenu. Na pia walisema: Hii Qur'ani si chochote ila ni uwongo ulio tungwa tu. Na walio ikataa Qur'ani ilipo wajia walisema: Hii si chochote ila ni uchawi ulio wazi.

44 Na Mwenyezi Mungu hakuwateremshia Waarabu Vitabu vya mbinguni wavisome; wala hutukupata kuwapelekea Mwonyaji kabla yako wa kuwahadharisha na matokeo ya ukafiri wao.

45 Na kaumu zilizo tangulia ziliwakadhibisha Manabii wao. Na hawa washirikina wa kaumu yako hawajafikia hata sehemu moja katika kumi za nguvu na umadhubuti tulio wapa hao walio tangulia. Wakawakanusha Mitume wangu. Basi ilikuwaje ghadhabu yangu juu yao jinsi nilivyo wakasirikia!

46 Waambie: Mimi nakuamrisheni jambo moja tu - Msimame kwa ikhlasi ya kumtakasia Mwenyezi Mungu muache kufuata mitindo yenu ya zamani - katika kuchungua kwa kumsafia niya Mwenyezi Mungu, mkgigawika wawili-wawili, au mmoja-mmoja, muangalie kwa uadilifu na insafu. Kisha mfikiri khabari ya huyu mwenzenu, Muhammad, ambaye mmeishi naye na mnajua kuwa akili yake ni timamu. Huyu hana wazimu kwa kuliingia jambo hili. Yeye huyu si chochote ila ni Mwonyaji kwenu, anakuhadharisheni msije mkapata adhabu kali inayo kukabilini mbele yenu

47 Waambie makafiri: Ujira wowote nilio kutakeni juu ya kufikisha Ujumbe ni kwa maslaha yenu. (Yaani nyinyi mwongoke na mpate malipo kwa Mwenyezi Mungu.) Sina ujira ninao utaraji mimi ila kwa Mwenyezi Mungu. Naye ni Mwenye kuangalia na kuchungua kila kitu.

Mwenye kujua vyema yaliyo ghaibu.⁴⁸

49. Sema: Kweli imefika, na uwongo haujitokezi, wala haurudi.⁴⁹

50. Sema: Ikiwa mimi nimepotea, basi nimepotea kwa kudhuru nafsi yangu mwenyewe. Na ikiwa nimeongoka, basi ni kwa sababu ya kunifunulia Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Aliye karibu.⁵⁰

51. Na lau ungeli ona watapo babaika, basi hapana pa kukimbilia! Na watakamatwa mahala pa karibu.⁵¹

52. Na watasema: Tunaiamini! Lakini wataipata wapi kutoka huko mahala mbali?⁵²

53. Na hapo kabla yake waliikataa, na wakiyatupilia mbali maneno ya ghaibu kutoka mahali mbali.⁵³

54. Na watatiliwa kizuizi baina yao na hayo wanayo yatamani, kama walivyo fanyiwa wenzao zamani. Hakika hao walikuwa na shaka ya kutia wasiwasi.⁵⁴

48 Waambie: Hakika Mola wangu Mlezi huitupa Haki juu ya baat'ili (uwongo) ikauondoa. Na Yeye ndiye Mwenye kujua vyema ghaibu; hapana siri inayo fichikana kwake

49 Waambie: Uislamu umedhihiri, wala uwongo hauwezi kuwa ndio njia ya kuipinga Haki. Na hizo mbinu za zamani hazirejei tena.

50 Waambie: Nikiiacha Haki basi madhara ya hayo yataniangukia mwenyewe. Na nikiongoka basi nimeongozwa na Mola wangu Mlezi. Yeye ni Mwenye kusikia kauli yangu na kauli yenu. Yupo karibu nami, na karibu yenu.

51 Na lau kuwa utaona, ewe mwenye kuona, pale watapo fazaika makafiri kweli itapo dhihiri, basi hawatakuwa na pa kukimbilia. Na watachukuliwa wapelekwe kwenye Moto kutoka pahala karibu.

52 Na watasema, watapo iona adhabu: Tunaiamini Haki! Na vipi wao waipate Imani kwa wepesi huo kutoka pahala mbali na dunia ambayo wakati wake umekwisha pita?

53 Na ilhali wao walikwisha ikataa Haki kabla ya Siku hii, na wakavurumiza kwa dhana ya uwongo kutoka mahala palipo mbali na ukweli.

54 Patawekewa kizuizi baina yao na hayo wanayo yatamani ya Imani ya kuwafaa, kama walivyo fanyiwa wenzao wa kabla yao walipo amini baada ya kwisha wakati wake. Kwa sababu wote hao wote walikuwa katika kuifanyia Haki shaka inayo pelekea kutuhumiwa.

Sura 35 - Faat'ir

Utangulizi

Sura hii imefunguliwa kwa kumsifu Mwenyezi Mungu, Muumba mbingu na ardhi, bila ya ruwaza, Mwenye kuwafanya Malaika kuwa ni wajumbe wa kuwatuma kwa waja wake. Malaika hao wana mbawa za idadi namna mbali mbali. Fadhila yoyote anayo wapelekea watu hapana wa kuizuia; na anayo izuia hapana wa kuipeleka. Mwenyezi Mungu anawataka watu waikumbuke neema, kwani hapana muumba mwengine aliye pamoja naye wa kuwapa riziki, wala hapana mungu pamoja naye wa wao kumwendea. Na watu wamekanusha wito wako. Lakini wewe unayo mazingatio kwa yaliyo wapitia Mitume walio tangulia. Nawe unayo ya kukuliwaza kwa tulivyo ahidi kuwa watarejea kwetu. Na waajibu kwa watu wasidanganyike na dunia na mapambo yake. Na asiwadanganye Shet'ani. Na shauri yake ni fupi, haipindikii kuliko kuwapelekea hao wafwasi wake kwenye maangamizo. Na mwenye kumfuata atamwongoza ampeleke Motoni. Wala hawawi sawa, mwenye kumpambia Shet'ani vitendo vyake viovu, na aliye muacha. Iliyoy kuwa shani ya watu ni hiyo, basi usisikitike kwa kuto amini kwao. Kwani Mwenye kuyapeleka mwingu na akahuisha kwayo kilicho kufa, atawafufua wafu kwa ajili ya hisabu na malipo. Mwenye kutaka nguvu atafute nguvu kwa Mwenyezi Mungu. Na mwenye kutafuta nguvu kwa mwenginewe, atamdhalilisha. Na vitendo vya waja vinapanda kwendea kwake. Yeye, basi huvikubali vitendo vya Waumini, na huviangusha vitendo vya makafiri. Na dalili ya uweza wake kufufua na kukusanya Siku ya Kiyama, ni kuwa kamuumba mwanaadamu kutokana na udongo kisha kutokana na tone la manii, tena akawafanya mwanamume na mwanamke. Wala mwanamke hachukui mimba wala hazai ila kwa ujuzi wake. Ameumba utamu na chumvi, na katika vyote hivyo unapata riziki. Na akauingiza usiku katika mchana, na mchana katika usiku. Na akafanya jua na mwezi yat'ii, kila kimoja wapo kinakwenda kwa muda maalumu. Muweza huyu ndiye Mungu wa Haki. Na hao wanao waomba badala yake hawamiliki, na wakiitwa hawasikii, na wakisikia hawajibu. Na Siku ya Kiyama hao wataukataa ushirikina walio washirikisha na Mwenyezi Mungu. Na Yeye ni Muadilifu, anambebesha kila mtu a'mali yake. Na wanaelekezwa Mitume wawakusudie kwa wito wao wale wanao mwogopa Mwenyezi Mungu. Na kazi ya Mtume ni kuwaonya watu wake. Na hapana umma wowote ila ulipitiwa na Mwonyaji. Sura tena inarejea kwenye dalili za uweza, kudra ya Mwenyezi Mungu. Kwa maji yanatokea mazao ya kila namna, na katika mawe ya majabali yapo namna mmbali mbali, nyeupe, nyekundu na nyeusi. Na watu na wanyama pia zinakhitalifiana rangi zao. Yote hayo yanapelekea kumnyenyekea Mwenyezi Mungu. Na mwenye kusoma kitabu cha Mwenyezi Mungu alichio mrithisha aliye mteuwa ataingia Peponi astarehe humo. Na mwenye kukufuru ataingia Motoni, hakuna mwisho huko, wala kupunguziwa adhabu yake. Atataka arejewe duniani ili atengeneze vitendo vyake, naye alikwisha pewa muhula wa kukumbuka lau kuwa ni mwenye kukumbuka. Na aliwajia Mwonyaji. Na Yeye, *Subhanahu* amekufanyeni ni warithi wa walio tangulia katika ardhi. Naye anaizuia mbingu isiondoke. Na wenye inadi waliapa kwamba akiwajia Mwonyaji hapana shaka watakuwa waongofu zaidi kuliko wlio watangulia. Alipo wajia wakatakabari, basi vitimbi vyao vikawaangukia wenyewe.

Na wao hawakumkadiria Mwenyezi Mungu anavyo stahiki kukadiriwa. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli wachukulia watu wa duniani kwa wanayo yafanya asingeli mwacha mnyama yoyote. Lakini anaakhirisha mpaka muda wao. Ukifika basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona waja wake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi, aliye wafanya Malaika kuwa wajumbe wenye mbawa, mbili-mbili, na tatu- tatu, na nne-nne. Huzidisha katika kuumba apendavyo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.¹
2. Rehema ambayo Mwenyezi Mungu anawafungulia watu hapana wa kuizua. Na anayo izuia hapana wa kuipeleka isipo kuwa Yeye. Naye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.²
3. Enyi watu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu. Ati yupo muumba mwengine asiye kuwa Mwenyezi Mungu anaye kupeni riziki kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Hapana mungu ila Yeye tu. Basi wapi mnako geuzwa?³
4. Na wakikukanusha, basi walikwisha kanushwa Mitume kabla yako. Na mambo yote yatarudishwa kwa Mwenyezi Mungu.⁴
5. Enyi watu! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala mdanganyifu asikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu.⁵
6. Hakika Shet'ani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui. Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni.⁶

1 Anaye stahiki sifa njema ni Mwenyezi Mungu peke yake. Yeye ndiye aliye zifanya mbingu na ardhi zikawa bila ya kuwapo ruwaza ya kuigia mfano wake. Naye ndiye aliye wajaalia Malaika kuwa ni wajumbe kuwatuma kwa viumbe vyake. Wao hao wana mbawa za idadi mbali mbali, mbili-mbili, tatu-tatu, na nne-nne. Yeye huzidisha katika kuumba kwake kama atakavyo kuzidisha. Hashindwi na kitu. Hakika Mwenyezi Mungu ana uweza mkubwa juu ya kila kitu.

2 Mwenyezi Mungu akipeleka rehema kwa watu, rehema yoyote ile iwayo, ikiwa ni mvua, au neema, au amani, au hikima - hapana mtu yeyote awezaye kuwazuilia na kuwanyima. Na chochote katika hivyo akikizuilia Yeye basi hapana mmoja awezaye kukifungulia isipo kuwa Yeye Mwenyewe. Na Yeye ndiye Mwenye kushinda ambaye hashindwi. Mwenye hikima asiye kosea.

3 Enyi watu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilio juu yenu, kwa kuzishukuru na kutimiza haki yake. Na mkiri hayo yaliyo tokea ndani ya nafsi zenu, ya kwamba hapana muumba isipo kuwa Mwenyezi Mungu ambaye anakuruzukuni kutoka mbinguni kwa zinavyo viteremsha, na kutoka kwenye ardhi kwa vinavyo toka humo, ambavyo vinakuleteeni uhai wenu. Hapana mungu isipo kuwa Yeye anaye waruzuku waja wake. Basi yawaje mnavyo geuzwa mkaacha Tawhidi ya Muumba wenu na Mwenye kukuruzukuni mkaendea kumshirikisha katika ibada yake?

4 Na hao makafiri wa kaumu yako wakikukadhabisha kwa uwongofu ulio waletea, basi wewe wastahamilie. Kwani Mitume wa kabla yako walikwisha kadhibishwa vile vile, na wakavumilia kwa walivyo kadhibishwa mpaka wakashinda. Na mambo yote yatarejea kwa Mwenyezi Mungu peke yake.

5 Enyi watu! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu, juu ya mambo ya kufufuliwa, na malipo, na ushindi, ni haki ya kweli. Basi msiache dunia ikakukhadaini na Akhera. Wala Shetani akakukhadaini mkaacha kuwafuata Mitume, na akakupeni tamaa kuwa mtasamehewa na hali huku mnaendelea na maasi.

6 Hakika Shetani ni adui yenu wa kale, msikhadaike kwa ahadi zake. Nanyi mchukulieni kuwa ni adui yenu. Kwani hakika yeye anawaita wafwasi wake wapate kuwa watu wa Moto uwakao kwa nguvu, na

7. Walio kufuru watakuwa na adhabu kali; na walio amini na wakatenda mema watapata msamaha na ujira mkubwa.⁷

8. Je! Yule aliye pambiwa a'mali zake mbaya na akazona ni njema - basi hakika Mwenyezi Mungu humwacha akapotea amtakaye, na humwongoa amtakaye. Basi nafsi yako isijihiliki kwa kuwasikitikia. Hakika Mwenyezi Mungu anajua wanayo yafanya.⁸

9. Na Mwenyezi Mungu ndiye anaye zituma Pepo ziyatimue mawingu, nasi tukayafikisha kwenye nchi iliyo kufa, tukaifufua ardhi baada ya kufa kwake. Ndivyo kama hivyo kutakavyo kuwa kufufuliwa.⁹

10. Mwenye kutaka utukufu basi utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye hupanda neno zuri, na a'mali njema Yeye huitukuza. Na wanao panga vitimbi vya maovu watapata adhabu kali. Na vitimbi vya hao vitaondokea patupu.¹⁰

11. Na Mwenyezi Mungu amekuumbeni kutokana na udongo. Kisha kwa tone la manii. Kisha akakufanyeni mwanamume na mwanamke. Na mwanamke yeyote hachukui mimba, wala hazai, ila kwa ilimu yake. Na wala hapewi umri mwenye umri mrefu, wala hapunguziwi katika umri wake, ila yamo hayo katika Kitabu. Hakika hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.¹¹

12. Na bahari mbili haziwi sawa; haya ni matamu yenye ladha, mazuri kunywa. Na haya ni ya chumvi, machungu. Na kutokana na bahari zote mnakula nyama mpya (isiyo chacha). Na mnatoa mapambo mnayo yavaa. Na unaona ndani yake marikebu zinakata maji ili mtafute fadhila zake, na ili mpate kushukuru.¹²

wala hawaitii kwa jenginele.

7 Wanao mkufuru Mwenyezi Mungu na Mitume wake watapata adhabu kali. Na wanao muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wakatenda mema watapewa kutokana na Mwenyezi Mungu kusamehewa madhambi yao, na ujira mkubwa kwa vitendo vyao.

8 Wamekuwa hawatambui? Je! Yule ambaye Shetani kampambia vitendo vyake viovu na mwenyewe akaona ni vizuri, ni kama aliye hidika kwa uwongofu wa Mwenyezi Mungu na akaliona jema kuwa ni jema, na uovu akauona kuwa ni uovu? Kwani hakika Mwenyezi Mungu humwacha akapotea amtakaye katika wanao khiari njia ya upotovu, wakaiona ndiyo njia ya kuifuata. Na humhidi amtakaye miongoni mwa walio ikhiari njia ya hidaya kuwa ndiyo njia ya kuifuata. Basi usihiliki nafsi yako kwa kuwasikitikia wapotovu na kuwaonea huruma. Hakika Mwenyezi Mungu anajua uovu wautendao, naye atawalipa kwa hayo.

9 Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anaye zituma pepo ziyatimue mawingu yaliyo rindika kwa mvuke wa maji. Tena tukayasukuma hayo mawingu mpaka kwenye nchi yenye ukame, tukaihuisha ardhi yake baada ya kuwa ilikuwa imekufa. Kama tunavyo itoa mimea katika ardhi, basi hali kadhaalika tutawatoa maiti makaburini Siku ya Kiyama. (*Rejea maoni ya ki-ilmu juu ya Aya 57 katika Sura ya 7, Al-Aa'raaf*)

10 Mwenye kutaka utukufu na nguvu na akazitafute kwa kumt'ii Mwenyezi Mungu. Kwani Yeye ndiye Mwenye nguvu zote. Kumwendea Yeye ndio linapanda neno jema. Na Mwenyezi Mungu huinyanyua a'mali njema na akaipokea. Na wale wanao wapangia Waumini vitimbi vya kuwadhuru watapata adhabu iliyo kali. Na hizo njama zao zitafisidika, hazito leta hayo waliyo yakusudia, wala hazileti natija yoyote.

11 Na Mwenyezi Mungu amekuumbeni kutokana na udongo. Kwani ndivyo hivyo alivyo muumba baba yenu Adam. Kisha akakuumbeni kutokana na tone ya manii, nayo ni maji yanayo miminwa katika tumbo la uzazi, nayo pia ni katika chakula kinacho toka kwenye udongo. Kisha akakufanyeni waume na wake. Wala mwanamke hachukui mimba, wala hazai ila kwa ujuzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wala hauongezwi umri wa mtu yeyote, wala haupunguzwi ila husajiliwa katika Kitabu. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni sahali, mepesi.

12 Na haziwi sawa bahari mbili katika ujuzi wetu na makadirio yetu, ijapo kuwa zinashirikiana katika baadhi ya manufaa yao. Haya maji matamu yanakata kiu kwa uzuri wake, na utamu wake, na wepesi wake kuyanywa. Na haya mengine ni maji ya chumvi, uchumvi wake mkali. Na kutokana na namna zote

13. Anauingiza usiku katika mchana, na anauingiza mchana katika usiku. Na amelifanya jua na mwezi kutumikia. Kila kimojapo kinakwenda kwa muda maalumu. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Ufalme ni wake. Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende.¹³

14. Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni. Na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu. Na hapana atakaye kupa khabari vilivyo kama Yeye Mwenye khabari.¹⁴

15. Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitoshia, Msifiwa.¹⁵

16. Akitaka atakuondoeni na alete viumbe vipya.¹⁶

17. Na hilo si gumu kwa Mwenyezi Mungu.¹⁷

18. Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine. Na aliye topewa na mzigo wake akiomba uchukuliwe hautachukuliwa hata kidogo, na angamwomba jamaa yake. Hakika wewe unawaonya wale wanao mcha Mola wao Mlezi kwa ghaibu, na wanashika Sala. Na anaye jitakasa, basi anajitakasa kwa ajili ya nafsi yake. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.¹⁸

19. Na kipofu na mwenye kuona hawalingani.¹⁹

mbili mnakula nyama mpya (fresh, haikuchacha) nayo ni samaki mnao wavua. Na mnatoa kutoka maji ya chumvi mapambo mnayo yavaa, kama lulu na marijani. Na wewe, mwenye kutazama, unaona vipi vyombo vya baharini vinavyo kwenda, vikipasua maji kwa mwendo wake, ili mkatafute baadhi ya fadhila za Mwenyezi Mungu kwa kufanya biashara, na ili asaa mpate kumshukuru Mola wenu Mlezi kwa neema hizi. (*Tazama Maelezo 35:12*)

13 Yeye huingiza usiku katika mchana, na mchana katika usiku. Matokeo yake ni kuwa saa zao hurefuka na hufupika kwa mujibu wa mipango ya hikima miaka nenda miaka rudi. Na Yeye amelifanya jua na mwezi kutumika kwa manufaa yenu. Kila kimojapo kinakwenda kwa muda maalumu utao ishia kwake. Huyo mwenye shani kuu ndiye Mwenyezi Mungu Mwenye kuyapanga mambo yenu. Ufalme ni wake Yeye peke yake. Na hao wengineo mnao waomba kuwa ni miungu mnao waabudu hawawezi kumiliki hata ugozi mwembamba ule wa kokwa ya tende. Basi inakuwaje wastahili kuabudiwa. (*Tazama Maelezo 35:13*)

14 Mkiwaomba hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu hawasikii maombi yenu. Na hata ingeli kuwa wanasikia wasingeli kujibuni kitu chochote kwa hayo myatakayo. Na Siku ya Kiyama watakuja kukataa huo ushirikina wenu kuwashirikisha na Mwenyezi Mungu. Wala hapana wa kukupeni khabari za hali za Akhera kuliko huyo Mwenye kujijua vyema kwa ujuzi wa ndani kabisa.

15 Enyi watu! Nyinyi ndio mnao mhitajia Mwenyezi Mungu kwa kila kitu. Na Yeye Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kujitoshia, hawahitajii viumbe vyake. Na Yeye ndiye Mwenye kustahiki kusifiwa kwa kila hali.

16 Mwenyezi Mungu akitaka kukuteketezeni, basi atakuteketezeni kwa utimilivu wa uweza wake. Na alete uumbaji mpya utao ridhiana na hikima yake.

17 Wala kukuhilikini nyinyi na kuwaleta wenginewe si muhali kwa Mwenyezi Mungu.

18 Wala nafsi yenye dhambi haitobeba dhambi za mwenginewe. Na mtu aliye kuwa taabani kwa mzigo wake wa madhambi, akimwomba mwenginewe amchukulie, huyo mwingine hatomchukulia hata kidogo, hata angeli kuwa ni jamaa yake. Haya ni kwa kuwa kila mtu kashughulika na yake. Na ewe Nabii! Usihuzunike kwa inadi ya watu wako. Kwani hakika maonyo yako yanawafaa wale ambao wanamkhofu Mola wao Mlezi peke yao katika siri, na wakashika Sala kwa mujibu inavyo faa. Na mwenye kujisafisha na uchafu wa madhambi, basi anajisafisha kwa faida ya nafsi yake. Na marejeo yote mwishoni ni kwa Mwenyezi Mungu, na Yeye atamtendea kila mtu kwa anavyo stahiki.

(*Rejea maoni ya ki-ilimu juu ya Aya 7 Sura ya 39, Azzumar: Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine*)

19 Hawawezi kulingana wakawa sawa:- asiye hidika kuifuata Haki kwa ujinga wake na mwenye kufuata Njia ya uwongofu kwa ujuzi wake; wala uwongo na kweli; wala kivuli na upepo umoto.

20. Wala giza na mwangaza.²⁰
21. Wala kivuli na joto.²¹
22. Wala hawalingani walio hai na maiti. Hakika Mwenyezi Mungu humsikilizisha amtakaye. Wala wewe si wa kuwasikilizisha walio makaburini.²²
23. Hukuwa wewe ila ni mwonyaji.²³
24. Hakika Sisi tumekutuma wewe kwa Haki, kuwa ni mbashiri na mwonyaji. Na hapana umma wowote ila ulipata mwonyaji kati yao.²⁴
25. Na wakikukanusha basi walikwisha wakanusha walio kuwa kabla yao. Mitume wao waliwajia kwa dalili wazi wazi na kwa maandiko na Kitabu chenye nuru.²⁵
26. Kisha nikawakamata walio kufuru. Basi kuchukia kwangu kulikuwaje?²⁶
27. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mbinguni, na kwayo tumeyatoa matunda yenye rangi mbali mbali. Na katika milima imo mistari myeupe na myekundu yenye rangi mbali mbali, na myeusi sana.²⁷
28. Na katika watu, na wanyama, na mifugo, pia rangi zao zinakhitalifiana. Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kusamehe.²⁸
29. Hakika wale wanao soma Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na wakashika Sala, na wakatoa kwa siri na kwa dhaahiri katika tulivyo waruzuku, hao hutaraji biashara isiyo bwaga.²⁹
30. Ili Yeye awalipe ujira wao kwa ukamilifu, na awazidishie kutokana na fadhila zake.

20 Tazama tanbihi ya 19.

21 Tazama tanbihi ya 19.

22 Wala hawawezi kuwa sawa walio hai kwa kukubali Imani, na maiti ambao hawahisi kitu na nyoyo zao zimefungika na kuweza kusikia yaliyo kweli. Hakika Mwenyezi Mungu humhidi amtakaye asikie hoja kwa sikio la kukubali. Wala wewe, ewe Nabii, si mwenye kuwasikilizisha walio kufa kwa inadi yao na ukafiri wao, kama ilivyo kuwa huwasikilizishi walio makaburini.

23 Wewe huna jukumu ila la kufikisha Ujumbe na kuonya tu.

24 Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekutuma wewe uwafikishie watu wote hii Dini ya Haki, ukiwabashiria Pepo wenye kuamini, na ukiwaonya kwa adhabu ya Moto wanao ikataa hii Dini. Na hapana kaumu yoyote katika kaumu zilizo pita ila walijiwa na mtu kutokana na Mwenyezi Mungu wa kuwahadharisha na adhabu yake.

25 Na ikiwa kaumu yako wanakukadhibisha wewe basi walio kuwa kabla yao waliwakadhibisha Mitume wao vile vile. Na wao waliwaletea miujiza iliyo wazi, na Maandiko ya Mola Mlezi na Kitabu chenye nuru kwa ajili ya kuwaongoza Njia ya kuokoka duniani na Akhera.

26 Kisha nikawashika walio kufuru kwa mshiko mkali. Basi hebu angalia kulikuwaje kuchukia kwangu kwa vitendo vyao, na ghadhabu yangu juu yao!

27 Ewe mwenye akili! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu anayateremsha maji kutoka mbinguni, na kwa maji hayo anatoa mazao yanayo khitalifiana rangi zake? Mengine ni mekundu na manjano, na matamu na machungu, mazuri na mabaya. Na katika milima, ipo milima yenye njia na mistari myeupe na myekundu, yenye kukhitalifiana pia kwa kukoza na kufifia. (*Tazama Maelezo 35:27*)

28 Na miongoni mwa watu na wanyama, na mifugo, yaani ngamia, ng'ombe, kondoo na mbuzi, kadhaalika zipo khitalifu katika sura, ukubwa na rangi. Na hawazingatii huu muumbo wa ajabu na wakamwogopa aliye umba ila wanazuoni ambao wanatambua siri ya uumbaji wake. Hakika Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda anaogopwa na Waumini, naye ni Mwingi wa kuwafutia madhambi yao wanao rejea kwake. (*Tazama Maelezo 35:28*)

29 Hakika wanao soma Kitabu cha Mwenyezi Mungu, kwa kukizingatia na kukitenda, na wakashika Sala kwa mujibu itakikanavyo na wakatoa kwa siri na kwa kuonekana baadhi ya alichu waruzuku Mwenyezi Mungu, wanataraji kwa hayo kufanya na Mwenyezi Mungu biashara isiyo anguka faida yake.

Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye shukrani.³⁰

31. Na hayo tuliyo kufunulia kutoka Kitabuni ni Kweli yenye kusadikisha yaliyo kuwa kabla yake. Hakika Mwenyezi Mungu kwa waja wake ni Mwenye khabari na Mwenye kuona.³¹

32. Kisha tumewarithisha Kitabu hao ambao tuliwateuwa miongoni mwa waja wetu. Kati yao yupo aliye jidhulumu nafsi yake, na yupo wa katikati, na yupo aliye tangulia katika mambo ya kheri, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo fadhila kuu.³²

33. Mabustani ya milele watayaingia. Huko watavikwa vikuku vya dhahabu, na lulu, na nguo zao humo ni za hariri.³³

34. Na watasema: *Alhamdulillah*, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliye tuondolea huzuni zote. Hakika Mola wetu Mlezi bila ya shaka ni Mwenye kusamehe, Mwenye shukrani.³⁴

35. Ambaye kwa fadhila yake ametuweka makao ya kukaa daima; humu haitugusi taabu wala humu hakutugusi kuchoka.³⁵

36. Na walio kufuru watakuwa na Moto wa Jahannamu, hawahukumiwi wakafa, wala hawatapunguziwa adhabu yake. Hivyo ndivyo tunavyo mlipa kila mwenye kuzidi ukafiri.³⁶

37. Na humo watapiga makelele: Mola wetu Mlezi! Tutoe tufanye mema sio yale tuliyo kuwa tukiyafanya. Kwani hatukukupeni umri wa kutosha kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Mwonyaji? Basi onjeni! Kwani walio dhulumu hawana wa kuwanusuru.³⁷

38. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa siri za mbinguni na ardhi. Hakika Yeye

30 Ili Mwenyezi Mungu awalipe ujira wao, na awazidishie juu yake kutokana na fadhila yake kwa anavyo waongezea mema yao na kuwafutia maovu yao. Yeye ni Msamehevu, Mwingi wa kufutia makosa ya kujikwaa, Mwenye kushukuru, Mwingi wa kushukuru kwa ut'iifu wa waja.

31 Na tuliyo kuletea Wahyi wewe katika hii Qur'ani ni Haki tupu isiyo kuwa na shaka yoyote. Tumeiteremsha kuthibitisha Vitabu vilivyo teremshwa kwa Mitume walio kuwa kabla yako, kwa kuwa vyote ni asli moja. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa kujua na kuona kwa waja wake.

32 Tena tumekifanya Kitabu hichi ni mirathi ya kurithiwa na waja wetu tulio wateuwa. Basi kati yao yupo aliye jidhulumu nafsi yake kwa kuzidi maovu yake kuliko mema yake; na yupo wa kiasi, hakupita mpaka katika maovu yake na wala hakukithirisha mema yake; na miongoni mwao yupo aliye washinda wengine kwa kufanya mambo ya kheri, kwa kusahilishiwa na Mwenyezi Mungu. Huko kushinda katika mambo ya kheri ndio kufuzu kukubwa mbele ya Mwenyezi Mungu,

33 Malipo yao Akhera ni Mabustani ya daima watayo yaingia. Humo watajipamba kwa vikuku vya dhahabu na lulu. Na nguo zao za Peponi ni hariri.

34 Na watasema wakisha ingia: Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu aliye tuondolea ya kutuhuzunisha. Hakika Mola wetu Mlezi ni Mwingi wa maghfira, Mwingi wa shukra.

35 Aliye tuweka kwenye Nyumba ya neema ya milele kwa fadhila zake hatupi taabu humo, wala hatuletei machofu.

36 Na walio kufuru malipo yao waliyo ahidiwa ni Moto wa Jahannamu watakuo uingia. Mwenyezi Mungu hatawahukumia mauti wakafa, wala hawatapunguziwa chembe ya adhabu wakapumzika. Ni kama hivyo tunavyo mlipa kila mwenye kuendelea katika ukafiri na akaushikilia.

37 Na humo watapiga makelele kuomba msaada wakisema: Mola wetu Mlezi! Tutoe humu Motoni, tupate kutenda mema siyo yale tuliyo kuwa tukiyatenda duniani. Atawaambia: Hatukukupeni fursa ya kufanya a'mali, tukaufanya mrefu umri wenu kwa muda unao mkinika mtu ndani yake kuzingatia kwa mwenye kuzingatia? Na akukujieni Mtume akakuhadharisheni na adhabu hii. Basi onjeni katika Jahannamu malipo ya udhalimu wenu. Kwani mwenye kudhulumu hapati wa kumnusuru wala kumsaidia.

ni Mjuzi wa yaliomo vifuani.³⁸

39. Yeye ndiye aliye kufanyeni manaibu katika ardhi. Na anaye kufuru, basi kufuru yake ni juu yake; na kufuru za makafiri haziwazidishii kwa Mola wao Mlezi ila kuchukiwa. Wala kufuru za makafiri haziwazidishii ila khasara.³⁹

40. Sema: Mnawaona hawa miungu wenu wa kishirikina mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu! Nionyesheni wameumba sehemu gani katika ardhi? Au wana ushirika wowote katika mbingu? Au tumewapa Kitabu nao kwa hicho wakawa na hoja zilizo wazi? Lakini madhaalimu hawaahidiani wao kwa wao ila udanganyifu tu.⁴⁰

41. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye anaye zulia mbingu na ardhi zisiondoke. Na zikiondoka hapana yeyote wa kuzizuia isipo kuwa Yeye. Hakika Yeye ni Mpole Mwenye kusamehe.⁴¹

42. Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa kuapa kwao, kwamba akiwajia mwonyaji bila ya shaka watakuwa waongofu zaidi kuliko taifa jingine lolote. Lakini alipo wajia mwonyaji hakuwazidishia ila kuikimbia hiyo Haki,⁴²

43. Kwa kutakabari kwao katika nchi, na kufanya vitimbi vya uovu. Na vitimbi viovu havimsibu ila mwenyewe aliye vifanya. Hebu hawangojei yalio wasibu watu wa kale? Basi hutapata mabadiliko katika mtindo wa Mwenyezi Mungu. Wala hutapata mageuko katika mwendo wa Mwenyezi Mungu.⁴³

44. Je! Hawakusafiri katika ardhi wakaona vipi ulikuwa mwisho wa walio kuwa kabla

38 Hakika Mwenyezi Mungu anajua vyema kila kilicho fichikana katika mbingu na ardhi. Hapana chenye kufichikana kwake. Na lau ange kukubalieni akakurudisheni duniani mngeli rejea yale yale aliyo kukatazeni. Hakika Yeye Mtukufu anavijua vyema vishawishi na vivutio viliomo ndani ya vifua.

39 Mwenyezi Mungu ndiye aliye kufanyeni baadhi yenu wawafuatie wengine katika kuiamirisha dunia na kuifanya itoe matunda yake. Na Yeye ni Mwenye kustahiki kushukuriwa si kukufuriwa. Basi mwenye kumkufuru Mwenyezi Mungu dhambi za kufuru yake zitakuwa juu yake mwenyewe. Na makafiri hawatopata ziada yoyote kwa Mola wao Mlezi isipo kuwa chuki na kukasirika. Wala makafiri hawatazidi ila kupata khasara tu.

40 Ewe Nabii! Waambie washirikina: Hebu nambieni, mmeiona hali ya hawa miungu wenu wa kishirikina mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu? Hebu nambieni, sehemu gani katika ardhi waliyo iumba wao? Hebu wanao ushirika wowote na Mwenyezi Mungu katika kuziumba mbingu? Sisi hatukuwapa kitabu cha ushirikina wakawa wao wanatoa hoja kutoka humo. Lakini wenye kuhulumu hawaahidiani wenyewe kwa wenyewe kwa uombezi wa miungu yao ya kumshirikisha na Mwenyezi Mungu ila kwa uwongo na kupambia pambia kuso mdanganya mtu ila aliye kuwa akili yake ni dhaifu.

41 Hakika Mwenyezi Mungu ndiye anaye zuia mpango wa mbingu na ardhi usivurugike, na ndiye anaye zihifadhi mbingu na ardhi zisiondoke. Na lau akizijaalia kuondoka hapana wa kuweza kuzihifadhi hizo isipo kuwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Hakika Yeye ni Mpole, hafanyi papara kuwaadhibu wakhalifu. Yeye ni Msamehevu wa madhambi ya wenye kurejea kwake wakatubu. (*Tazama Maelezo 35:41*)

42 Na makafiri waliapa kwa jina la Mwenyezi Mungu mwisho wa juhudi yao kutilia nguvu kiapo chao, ya kwamba bila ya shaka akiwajia Mtume kuwaonya basi wao hapana shaka watakuwa miongoni mwa mataifa walio ongoka zaidi kuliko hao wenginewe walio wakadhibisha Mitume wao. Lakini alipo wajia Mtume kutokana na wao wenyewe, akiwaonya, hakuwazidishia kwa kuwaonya kwake na kuwanasihi, isipo kuwa kuikimbia Haki.

43 Wameikimbia Haki kwa kupandwa na kiburi katika nchi, na kuona ari kumnyenyeka Mtume na Dini aliyo kuja nayo. Wakapanga njama za vitimbi viovu. Na ni Shetani ndiye aliye waongoza hata wakaiacha Dini na wakaingia kumpiga vita Mtume. Na wala madhara ya vitimbivi viovu hayampati mtu ila yule yule aliye vipanga. Basi watu hao wanangojea nini isipo kuwa sunna ya Mwenyezi Mungu iliyo wasibu wale walio watangulia? Basi hutoipata njia ya Mwenyezi Mungu anavyo yafanyia mataifa ibadilike, kama wanavyo tumai hawa wapangaji vitimbi yawe kinyume na walio watangulia. Na kabisa hutopata mwendo wa Mwenyezi Mungu ubadilishie njia ulio elekea.

yao? Na hao walikuwa wana nguvu zaidi kuliko wao. Na hapana kitu kinacho weza kumshinda Mwenyezi Mungu mbinguni wala katika ardhi. Hakika Yeye ni Mwenye kujua, Mwenye uweza.⁴⁴

45. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli wachukulia watu kwa waliyo yachuma, basi asingeli muacha juu ya ardhi hata mnyama mmoja. Lakini Yeye anawachukulia mpaka ufike muda maalumu. Basi ukifika muda wao basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona waja wake baraabara.⁴⁵

44 Je! hao hukaa na wakakanya tu ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa washirikina, bila ya wao kusafiri katika ulimwengu wakaangalia kwa macho yao athari za maangamizo yaliyo wateremkia walio kuwa kabla yao kwa sababu ya kuwakadhibisha kwao Mitume? Na kabla ya wao yalikuwako mataifa yaliyo kuwa na nguvu kushinda wao. Nguvu zao hazikuweza kuzuia adhabu ya Mwenyezi Mungu. Kwani Yeye hashindwi na chochote kilioko mbinguni wala katika ardhi. Hakika Yeye ni Mwenye ilimu kubwa kabisa, Mwenye uweza mkubwa kabisa

45 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli kuwa anawaadhibu watu duniani, basi hapana shaka adhabu yake ingeli enea. Na asingeli muacha juu ya mgongo wa ardhi hata mnyama mmoja, kwa kuwa wote wametenda madhambi. Lakini anaakhirisha kuwaadhibu mpaka siku maalumu, nayo ni Siku ya Kiyama. Basi ukifika muda wao walio wekewa atawalipa kwa uangalizi kaamili. Kwani Yeye ni Mwenye kuviona vitendo vya waja wake; hafichikiwi na kitu chochote katika hivyo. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua kushinda wote.

Sura 36 - Ya-Sin

Utangulizi

Sura hii imeanzia kwa harufi mbili ambazo ni katika harufi za kuundiwa maneno ya Kiarabu. Na ikafuatiliza kwa kuapa kwa Qur'ani ya kwamba Muhammad s.a.w. bila ya shaka ni miongoni mwa Mitume, walio tumwa. Na kuwa hakika yeye yuko kwenye Njia Iliyo Nyooka iliyo rasimiwa na Qur'ani aliyo teremshiwa yeye kutokana na Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu, ili apate kuwaonya kwayo watu ambao baba zao hawakupata kabla yake kuonywa. Tena Sura ikaingia kutufanyia taswira, picha, ya wanao kataa, ambao hawanafiiki na maonyo. Na inatubainishia kwamba kuonya humfaidisha mwenye kuelekea kupokea makumbusho, na kumcha Mwingi wa Rehema. Na kwamba hakika Mwenyezi Mungu atawafufua wafu, na atavihisabu vitendo vya waja. Na Sura ikaingilia kuwapigia mfano makafiri wa Makka, na ikabainisha mvutano baina ya wanao mlingania Mwenyezi Mungu na wanao kadhibisha. Inabainisha mwisho wa makundi mawili hayo. Kisha ikawa inaeleza dalili za uweza unao pasa kuuamini na kuogopa miadi ya Mwenyezi Mungu itakayo watokea ghafla katika Siku ambayo kila mtu atalipwa kwa aliyo yatenda. Watu wa Peponi watastareheshwa. Watapata wanacho kitamani. Na watu wa Motoni watafukuzwa. Nao watakuwa katika mbano wa uweza wa Mwenyezi Mungu. Midomo yao itazibwa, na viungo vyao ndivyo vitavyo tamka. Na Mwenyezi Mungu angeli penda, basi bila ya shaka angeli zigeuza sura zao pia. Kwani ni Yeye ndiye Mwenye kumbadilisha anaye mrefushia umri wake duniani badala ya nguvu akawa dhaifu, na badala ya akili akawa amepiswa. Na Yeye ndiye aliye mlinda Nabii wake na kuzugwa na kichaa. Naye hakumfundisha utungaji mashairi, na wala hauhitajiki ufundi huo unao mfanya aliye nao kutanga tanga katika kila bonde. Mtume hakuja ila kwa ajili ya ukumbusho ulio wazi, ulio tokana na akili, sio ulio tokana na mawazo mapepe tu. Na Sura ikaendelea kukumbusha fadhila za Mwenyezi Mungu juu ya waja wake, na kwamba Yeye amewafanya wanyama wa mifugo ambao wanawamiliki na wanawapanda wawatumikie. Na juu ya neema hizi zililo wekwa kwa faida yao, wao bado wanakwenda kuabudu miungu ya ushirikina isiyo weza kitu. Na Sura inakhitimisha kwa kumtaka binaadamu aangalie namna alivyo umbwa kutokana na tone la manii, na khalafu yeye anakuwa ni mpinzani wa kudhihirisha upinzani wake. Na yule aliye umbwa hapo mwanzo, na anaye toa moto kutoka mti wa kijani, na aliye umbwa mbingu na ardhi, huyo basi ni Muweza wa kuyafufua mafupa nayo yamekwisha vurugika. Na amri yake ni kukiambia kitu: Kuwa! Na kikawa. Ametakasika Mwenye kumiliki kila kitu. Na kwake Yeye mtarejea.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ya-Sin (Y.S.).¹

¹ Ya-Sin: Hizi ni harufi mbili zilizo anzia Sura hii kwa mujibu wa mpango wa Qur'ani katika kuanzia baadhi ya Sura kwa harufi moja moja.

2. Kwa Haki ya Qur'ani yenye hikima!²
3. Hakika wewe ni miongoni mwa walio tumwa,³
4. Juu ya Njia Iliyo Nyooka.⁴
5. Uteremsho wa Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.⁵
6. Ili uwaonye watu ambao baba zao hawakuonywa , basi wao wamekuwa wenye kughafilika.⁶
7. Bila ya shaka kauli imekwisha thibiti juu ya wengi katika wao, kwa hivyo hawaamini.⁷
8. Tumeweka makongwa shingoni mwao, yakawafika videvuni. Kwa hivyo vichwa vyao viko juu tu.⁸
9. Tumeweka kizuizi mbele yao, na kizuizi nyuma yao, na tumewafunika macho yao; kwa hivyo hawaoni.⁹
10. Ni sawa sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawataamini.¹⁰
11. Hakika wewe unamwonya mwenye kufuata ukumbusho, na akamcha *Arrahman*, Mwingi wa Rehema, kwa ghaibu. Basi mbashirie huyo msamaha na ujira mwema.¹¹
12. Hakika Sisi tunawafufua wafu, na tunayaandika wanayo yatanguliza, na wanayo yaacha nyuma. Na kila kitu tumekihifadhi katika daftari asli lenye kubainisha.¹²
13. Na wapigie mfano wa wakaazi wa mji walipo wafikia walio tumwa.¹³
14. Tulipo watumia wawili, wakawakanusha. Basi tukawazidishia nguvu kwa mwingine wa tatu. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwenu.¹⁴
15. Wakasema: Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi. Na Mwingi wa Rehema hakuteremsha kitu. Nyinyi mnasema uwongo tu.¹⁵

2 Ninaapa kwa Qur'ani yenye kukusanya hikima na ilimu yenye manufaa.

3 Hakika wewe, Muhammad, ni katika wale ambao Mwenyezi Mungu amewatuma kwa watu wawapelekee Uwongofu na Dini ya Haki.

4 Juu ya Njia Iliyo Sawa, nayo ndiyo Dini ya Kiislamu.

5 Ni mteremsho wa Mwenye nguvu Mwenye kushinda kila kitu, ambaye hapana mtu awezae kumzia chochote akitakacho. Mwenye kuwarehemu waja wake, kwa kuwatumia watu wa kuwaongoza njia ya kuokoka.

6 Ili uwaonye watu ambao baba zao wa karibu hawakupata kuonywa, na kwa hivyo wamesahau yanayo wajibikia kwa Mwenyezi Mungu, na kwa nafsi zao, na kwa watu

7 Sisi tulikwisha jua kuwa wengi wao hawatakiari Imani. Basi yale tuliyo kuwa tunayajua yamewafikiana na yaliyo kwao. Basi haitakuwapo Imani kutoka kwao.

8 Sisi tumewafanya hao wanao kakamia juu ya ukafiri ni kama walio tiwa minyororo shingoni mwao, ikawafika videvuni mwao. Na mikono yao ikawa imefungwa kwenye vichwa vyao, vikawa vimenyanyuka juu na macho yao yameinama. Basi hawawezi kuvizungusha vichwa vyao wapate kuona.

9 Na tumewafanya wale walio zuwiwa wasione Ishara na dalili ni kama walio fungwa baina ya kuta mbili, na macho yao yakagubikwa, wasione yaliyo mbele yao wala yaliyo nyuma yao.

10 Na ni sawa kwao ukiwahadharisha au ukito wahadharisha, hawaamini hao.

11 Hakika wanao nafiika kwa kuhadharisha kwako ni wale wanao ifuata Qur'ani na wakamkhofu *Arrahman*, ijapo kuwa hawamwoni. Basi watu hawa wape bishara njema kuwa Mwenyezi Mungu atawasamehe madhambi yao, na atawalipa malipo mema kwa vitendo vyao.

12 Hakika Sisi tunawahuisha maiti, na tunayaandika yote waliyo yatenda na wakayakadimisha duniani, na walio yabakisha humo kuwa ni athari, mabaki, yao baada ya kufa kwao. Na kila kitu kimo katika Kitabu kilicho wazi.

13 Ewe Nabii! Watajje watu wako kisa cha mji mmoja. Kwani hicho ni kama kisa chao. Waliwaendea Wajumbe walio tumwa ili wawahidi. (*Tazama Maelezo 36:13*)

14 Tuliwatuma wajumbe wawili, wakawakadhibisha. Tukawaongeza nguvu kwa kumpeleka mwengine wa tatu. Basi hawa watatu wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwenu!

15 Wale watu wa mji wakasema kuwajibu: Nyinyi si chochote ila ni wanaadamu kama sisi. Na Mwenyezi

16. Wakasema: Mola wetu Mlezi anajua kwamba hakika sisi tumetumwa kwenu.¹⁶
17. Wala si juu yetu ila kufikisha ujumbe ulio wazi.¹⁷
18. Wakasema: Sisi tumeagua kuwa nyinyi ni wakorofi. Ikiwa hamtaacha basi kwa yakini tutakupigeni mawe, na mtapata adhabu chungu kutoka kwetu.¹⁸
19. Wakasema: Ukorofi wenu mnao wenyewe! Je! Ni kwa kuwa mnakumbushwa? Ama nyinyi ni watu walio pindukia mipaka.¹⁹
20. Na akaja mtu mbio kutokea upande wa mbali wa mjini, akasema: Enyi watu wangu! Wafuateni hawa walio tumwa.²⁰
21. Wafuateni ambao hawakutakini ujira, hali ya kuwa wenyewe wameongoka.²¹
22. NA KWA NINI nisimuabudu yule aliye niumba na kwake mtarejeshwa?²²
23. Je! Niishike miungu mingine badala yake? *Arrahmani*, Mwingi wa Rehema, akinitakia madhara uombezi wa hao hautanifaa kitu, wala hawataniokoa.²³
24. Basi hakika mimi hapo nitakuwa katika upotovu ulio dhaahiri.²⁴
25. Hakika mimi nimemuamini Mola wenu Mlezi, basi nisikilizeni!²⁵
26. Akaambiwa: Ingia Peponi! Akasema: Laiti kuwa watu wangu wangeli jua²⁶
27. Jinsi Mola wangu Mlezi alivyo nisamehe, na akanifanya miongoni mwa walio hishimiwa.²⁷
28. Na hatukuwateremshia kaumu yake baada yake jeshi kutoka mbinguni, wala si wenye kuteremsha.²⁸
29. Hakukuwa ila ukelele mmoja tu; na mara walizimwa!²⁹

Mungu Mwingi wa Rehema hakuteremsha wahyi wowote kwa mwanaadamu. Nyinyi ni watu mnao sema yasiyo kuwapo.

16 Wale Wajumbe wakasema: Mola wetu Mlezi aliye tutuma anajua kuwa hakika sisi bila ya shaka tumetumwa kwenu.

17 Na sisi hatuna waajibu wowote ila kufikilisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu ufike kwa uwazi.

18 Wana mji wale wakasema: Sisi tunaona kuwa nyinyi mnatuletea ukorofi. Na tunaapa, lau kuwa hamsiti na huo wito wenu hapana shaka tutakupopoeni kwa mawe, na hapana shaka mtapata kwetu adhabu kali yenye kutia uchungu.

19 Wale Wajumbe wakasema: Ukorofi mnao nyinyi wenyewe, kwa hizo kufuru zenu. Badala ya kuwaidhika kwa mambo yenye kheri kwenu wenyewe, mnatutuhumu sisi kuwa ni wakorofi, na mnatutishia kutupa adhabu chungu? Lakini nyinyi ni watu mlio pindukia mipaka ya Haki na Uadilifu.

20 Akaja mtu kutoka huko mwisho wa mji akiwakimbilia wale wanamji, akawaambia: Wafuateni hawa walio tumwa kwenu na Mwenyezi Mungu.

21 Wafuateni watu wasio taka kwenu ujira wowote kwa kukunasihini na kukuongozeni, na hali wao wenyewe wameongoka, na nyinyi mtapata manufaa kwa kufuata njia ya kheri na mafanikio!

22 Na kitu gani cha kunizuia hata nisimuabudu yule aliye niumba, na ambaye kwake Yeye, si kwa mwenginewe, ndio mtarejea?

23 Je! Niishike kwa kuiabudu badala ya Mwenyezi Mungu, miungu mingine isiyo nifaa kitu kuniombea kwao, pindi Mwenyezi Mungu akinitakia madhara? Wala hawataniokoa nayo yakinishukia hayo madhara.

24 Basi hakika mimi nikiabudu miungu mingine badala yake Yeye, nitakuwa katika upotovu ulio dhaahiri.

25 Hakika mimi ninamsadiki Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni, na ndiye Mwenye kutawala mambo yenu. Basi nisikilezeni na mnit'ii.

26 Kuwa ni malipo ya Imani yake na wito wake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ataambiwa: Ingia Peponi! Naye, hali yuko katika kivuli cha neema na hishima, atasema: Laiti kuwa watu wangu wangeli jua alivyo nighufiria Mola wangu Mlezi na kunipa hishima, nao wakaamini kama nilivyo amini mimi.

27 Tazama tanbihi ya 26.

28 Na Sisi hatukawaangamiza kwa kuwapelekea maaskari kutoka mbinguni. Wala huo sio mtindo wetu kupeleka majeshi tunapo yahiliki mataifa.

29 Kuteketezwa kwao hakukuwa ila ni kwa ukelele mmoja tu tulio wapelekea. Na mara wao wakawa ni

30. Nawasikitikia waja wangu. Hawajii Mtume ila wao humkejeli.³⁰
31. Je! Hawaoni umma ngapi tulizo ziangamiza kabla yao? Hakika hao hawarejei tena kwao.³¹
32. Na hapana mmoja ila wote watakusanywa waletwe mbele yetu.³²
33. Na Ishara hiyo kwao - ardhi iliyo kufa, nasi tukaifufua, na tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila!³³
34. Na tukafanya ndani yake mabustani ya mitende na mizabibu, na tukatimbia chemchem ndani yake,³⁴
35. Ili wale matunda yake, na hayo hayakufanywa na mikono yao! Basi je, hawashukuru?³⁵
36. *Subhana*, Ametakasika, aliye umba dume na jike vyote katika vinavyo mea katika ardhi na katika nafsi zao, na katika wasivyo vijua.³⁶
37. Na usiku ni Ishara kwao. Tunauvua humo mchana, mara wao wanakuwa gizani.³⁷
38. Na jua linakwenda kwa kiwango chake. Hayo ni makadirio ya Mwenye nguvu, Mwenye kujua.³⁸
39. Na mwezi tumeupimia vituo, mpaka unakuwa kama karara kongwe.³⁹
40. Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaoagelea katika njia zao.⁴⁰
41. Na ni Ishara kwao kwamba Sisi tuliwapakia dhuriya zao katika jahazi ilio sheheni.⁴¹

maiti, kama moto ulio zimwa.

30 Ee khasara yao, inayo faa kusikitikiwa! Hatuwapelekei waja wangu Mtume ila wao huwa wakimfanyia maskhara.

31 Kwani wao hawayazingatii mataifa mengi yaliyo tangulia tuliyo yahiliki? Hakika hao hawarejei tena kwenye maisha yao ya duniani.

32 Hapana katika mataifa yaliyo tangulia na yajayo ila wote watakusanywa mbele yetu, nao wamelazimishwa kuhudhuria mbele yetu.

33 Na dalili kwao ya uweza wetu wa kufufua ni kuangalia vipi ardhi yenye ukame tunavyo ihuisha kwa maji, na kutoa ndani yake nafaka wanazo zila.

34 Na humo tukafanya vitalu na mabustani ya mitende na mizabibu, na tukapasua humo chemchem ya kumwagia maji kwenye miti yake, na ikatoa matunda, na wao wakala katika hayo. Na hayo si kazi ya mikono yao. Basi kwa nini hawatoi haki ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yao kwa kumuamini na kumshukuru?

35 Tazama tanbihi ya 34.

36 Wa kutakasika ni Mwenyezi Mungu aliye umba kila kitu kwa mpango wa ume na uke, katika mimea na katika nafsi zao watu, na katika vitu ambavyo watu hawavijui. (*Tazama Maelezo 36:36*)

37 Na Ishara pia ya kuwepo Mwenyezi Mungu na uweza wake, ni huu usiku ambao tunautoa ndani yake mchana, kama kuivua nguo inayo sitiri. Mara utaona watu wamo gizani lililo wazunguka kila upande.

38 Na jua linakwenda katika njia yake maalumu. Mwenyezi Mungu amekwisha kadiria kwa zama na mahala. Huo ndio mpango wake Mwenye kushinda kwa uweza wake, Mwenye kuvizunguka vitu vyote kwa ujuzi wake.

39 Na mwezi kwa mpango wetu tumeujaalia una vituo vyake. Mwanzo wa mwezi unakuwa mdogo na mwembamba. Kisha kila usiku unazidi kukua mpaka unatimia kuwa mbaamwezi. Tena unaingia kupungua vile vile, mpaka ukawa kama karara la mtende linapo kuwa kongwe limepindana na limekuwa manjano.

40 Haipelekei jua likaacha sharia zake likakutana na mwezi, na likaingia katika njia zake. Wala usiku hauwi kuushinda mchana ukauzuia usije, bali vyote viwili hivyo hupeana zamu. Na vyote, jua na mwezi, na vyenginevyo vyote vinaoagelea katika njia zao za mbinguni, wala haviachi njia. (*Tazama Maelezo 36:40*)

41 Na Ishara nyengine kwao ni kuwa Sisi tuliwapakia wanaadamu katika jahazi ilio jaa bidhaa zao na riziki zao.

42. Na tukawaambia kutoka mfano wake wanavyo vipanda.⁴²
43. Na tukitaka tunawazamisha, wala hapana wa kuwasaidia, wala hawaokolewi,⁴³
44. Isipo kuwa kwa rehema zitokazo kwetu na starehe kwa muda.⁴⁴
45. Na wanapo ambiwa: Jilindeni na yalioko mbele yenu na yalioko nyuma yenu, ili mpate kurehemewa.⁴⁵
46. Na haiwafikii Ishara yoyote katika Ishara za Mola wao Mlezi ila wao huwa ni wenye kuipuuza.⁴⁶
47. Na wanapo ambiwa: Toeni katika aliyo kupeni Mwenyezi Mungu, walio kufuru huwaambia walio amini: Je! Tualishe ambao Mwenyezi Mungu angependa angeli walisha mwenyewe? Nyinyi hammo ila katika upotofu ulio dhaahiri.⁴⁷
48. Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa nyinyi ni wakweli?⁴⁸
49. Hawangojei ila ukelele mmoja tu utakao wachukua nao wamo kuzozana.⁴⁹
50. Basi hawataweza kuusia, wala kwa watu wao hawarejei.⁵⁰
51. Na litapulizwa barugumu, mara watatoka makaburini wakikimbilia kwa Mola wao Mlezi.⁵¹
52. Watasema: Ole wetu! Nani aliye tufufua kwenye malazi yetu? Haya ndiyo aliyo yaahidi Mwingi wa Rehema na wakasema kweli Mitume.⁵²
53. Haitakuwa ila ukelele mmoja tu, mara wote watahudhuruishwa mbele yetu.⁵³
54. Basi leo nafsi yoyote haitadhulumiwa kitu, wala hamtalipwa ila yale mliyo kuwa mkiyatenda.⁵⁴

42 Na tukawaambia mfano wa hiyo marikebu na vyenginevyo wanavyo vipanda kadhaalika.

43 Na tukitaka kuwazamisha, tunawazamisha. Na wala hawapati wa kuwaopoa, wala hawapati wa kuwaokoa wasiangamie.

44 Lakini Sisi hatuwazamishi, kwa sababu ya rehema inayo tokana nasi, na ili tuwastareheshe kwa muda ulio kwisha kadiriwa.

45 Na wanapo ambiwa: Yaogopeni mfano wa yaliyo wapata mataifa yaliyo kwisha pita kwa kukadhibisha kwao, na iogopeni adhabu ya Akhera ambayo itakupateni kwa kushikilia kwenu ukafiri, kwa kutaraji kuwa asaa Mola wenu Mlezi akakurehemuni mkimcha Yeye, wao hupuuza.

46 Na haiwajii hoja katika hoja za Mola wao Mlezi, yenye kuonyesha Upweke wa Mwenyezi Mungu na uweza wake, ila wao huipa nyongo, hawaijali.

47 Na wakiambiwa: Wapeni mafakiri kutokana na hicho alichokuruzukuni Mwenyezi Mungu, makafiri huwaambia Waumini: Je! Tualishe watu ambao Mwenyezi Mungu Mwenyewe angeli taka angeli walisha? Hivyo inakuwa tunamfanyia inda Mwenyezi Mungu kwenda kinyume na mapenzi yake! Nyinyi mnao taka tutoe, si chochote ila mmo katika upofu ulio wazi, hamuioni Haki.

48 Na huwaambia Waumini kwa kuwafanyia kejeli: Lini yatatokea hayo mlio tuahidi, kama nyinyi mnasema kweli katika mnayo ahidi?

49 Hawangojei ila sauti moja tu, iwamalize kwa ghafla, nao wakizozana katika mambo ya kidunia, wameghafilika na Akhera.

50 Kwa upesi wa hayo yatakayo wateremkia, hawatowahi kuusia chochote, wala kurejea kwa ahali zao.

51 Na barugumu litapulizwa kwa mpulizo wa kufufua watu. Mara watu watatoka makaburini mwao wakikimbilia kwenda kukutana na Mwenyezi Mungu. Na hilo barugumu, na kupulizwa kwake, ni katika anayo yajua Mwenyezi Mungu Yeye peke yake.

52 Watasema watakapo fufuliwa kutoka makaburini: Balaa gani lilio tushukia! Nani aliye tuamsha tukauwacha usingizi wetu? Jawabu ya suala lao itawajia: Hii ndiyo siku ya kufufuliwa aliyo waahidia Arrahaman, Mwingi wa Rehema, waja wake, na Mitume wakaisemea kweli kwa waliyo yasimulia

53 Wito wao wa kuwatoa hautakuwa ila ukelele mmoja tu, mara wote watakusanywa mbele yetu wahudhurishwe ili tuwahisabie.

54 Basi katika hii siku ya leo haipungukiwi nafsi na chochote katika ujira wake kwa kazi iliyo tenda. Na wala hamtopata isipo kuwa jaza ya mliyo kuwa mkiyatenda, ikiwa ni kheri au shari.

55. Hakika watu wa Peponi leo wamo shughulini, wamefurahi.⁵⁵
56. Wao na wake zao wamo katika vivuli wameegemea juu ya viti vya fakhari.⁵⁶
57. Watapata humo kila namna ya matunda na watapata kila watakacho kitaka.⁵⁷
58. “Salama!” Hiyo ndiyo kauli itokayo kwa Mola Mlezi Mwenye kurehemu.⁵⁸
59. Na enyi wakosefu! Jitengeni leo!⁵⁹
60. Je! Sikuagana nanyi, enyi wanaadamu, kuwa msimuabudu Shet’ani? Hakika yeye ni adui dhaahiri kwenu.⁶⁰
61. Na ya kwamba mniabudu Mimi? Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka.⁶¹
62. Na bila ya shaka yeye amekwisha lipoteza kundi kubwa miongoni mwenu. Je, hamkuwa mkifikiri?⁶²
63. Hii basi ndiyo Jahannamu mliyo kuwa mkiahidiwa.⁶³
64. Ingieni leo kwa vile mlivyo kuwa mkikufuru.⁶⁴
65. Leo tunaviziba vinywa vyao, na iseme nasi mikono yao, na itoe ushahidi miguu yao kwa waliyo kuwa wakiyachuma.⁶⁵
66. Na tungeli penda tungeli yafutilia mbali macho yao, wakawa wanaiwania njia. Lakini wange ionaje?⁶⁶
67. Na tungeli taka tunge wageuza sura hapo hapo walipo, basi wasinge weza kwenda wala kurudi.⁶⁷
68. Na tunaye mzeesha tunamrudisha nyuma katika umbo. Basi je! hawazingatii?⁶⁸
69. Wala hatukumfundisha (Muhammad) mashairi, wala hayatakikani kwake hayo. Haukuwa huu ila ni ukumbusho na Qur’ani inayo bainisha.⁶⁹

55 Hakika watu wa Peponi hii leo watakuwa wameshughulika kwa neema walizo nazo, wakistaajabia na kufurahia.

56 Wao na wake zao wamo katika vivuli vilivyo enea, wameegemea juu ya viti vilivyo pambwa.

57 Watapata huko Peponi kila namna ya matunda, na kila wakitakacho watakipata.

58 Wataambiwa: “Salama”, kuwa ni kauli iliyo toka kwa Mola Mlezi Mwenye kurehemu.

59 Na wataambiwa wakosefu siku hii ya leo: Jitengeni mbali na Waumini.

60 Enyi wanaadamu! Sikukuusieni kuwa msimfuata Shetani kwa ut’ifu kama kwamba ni mungu wa kuabudiwa. Hakika yeye ni adui yenu, aliye dhihirisha uadui wake.

61 Na nyinyi mniabudu Mimi peke yangu, kwani kuniabudu Mimi tu ndiyo Njia kuu katika kusimamisha Dini sawa.

62 Na Shetani amewapotoa viumbe wengi kati yenu. Nyinyi mmeghafilika na hayo. Basi hamkuwa mkifikiri mlipo mt’ii yeye.

63 Wataambiwa: Hii ndiyo Jahannamu mliyo kuwa mkiahidiwa mlipo kuwa duniani. Ndiyo jaza ya ukafiri wenu.

64 Ingieni! Na hilikini kwa joto lake hii leo kwa ukafiri wenu!

65 Leo vitazibwa vinywa vyao, basi havito tamka kitu. Mikono yao ndiyo itakayo sema nasi, na miguu yao itatamka kwa kutoa ushahidi juu yao kwa waliyo kuwa wakiyafanya.

66 Na tungeli taka kuwatia upofu duniani tungeli watia upofu, wakawa wanaipapasa njia ya kupita wasiweze kuiona. Wataionaje nasi tumewapofoa!

67 Na lau tungeli taka kuzigeuza sura zao tungeli zigeuza zikawa mbaya, juu ya kuwa wana nguvu na vyeo. Hata wasinge weza kwenda mbele wala kurudi nyuma, kwa kuwa inge kuwa tumevunja nguvu zao.

68 Na tunaye mfanyia umri wake ukawa mrefu, tunamrudisha, kutoka nguvu akawa dhaifu. Basi je hawazingatii haya wakayatia akilini ya uweza wetu kuyafanya haya, na wao wakajua kuwa dunia ni nyumba ya kupita ina mwisho wake, na kuwa Akhera ndiyo nyumba ya kubaki na kudumu? (*Tazama Maelezo 36:68*)

69 Na Sisi hatukumfunza Mtume kutunga mashairi. Wala haifai hivyo, kwa kuzingatia pahala pake na cheo chake awe mtungaji mashairi! Hii Qur’ani iliyo teremka juu yake si chochote ila ni mawaidha, na Kitabu cha mbinguni kilio wazi. Hakikhusiani kabisa na mashairi.

70. Ili imwonye aliye hai, na neno litimie juu ya makafiri.⁷⁰
71. Je! Hawaoni kwamba tumewaumbia kutokana na iliyo fanya mikono yetu wanyama wa mifugo, na wao wakawa wenye kuwamiliki.⁷¹
72. Na Sisi tukawadhaliishia. Basi baadhi yao wako wanao wapanda, na baadhi yao wanawala.⁷²
73. Na wao wanapata kwao manufaa na vinywaji. Basi je, hawashukuru?⁷³
74. Na wameishika miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili ati wapate kusaidiwa!⁷⁴
75. Hawataweza kuwasaidia. Bali hao ndio watakuwa askari wao watakao hudhurishwa.⁷⁵
76. Basi maneno yao yasikuhuzunishe. Hakika Sisi tunayajua wanayo yaweka siri na wanayo yatangaza.⁷⁶
77. Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi tumemuumba yeye kutokana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa ndiye mgomvi wa dhaahiri!⁷⁷
78. Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakaye ihuisha mifupa nayo imekwisha mung'unyika?⁷⁸
79. Sema: Ataihuisha huyo huyo aliye iumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila kuumba.⁷⁹
80. Aliye kujaalieni kupata moto kutokana na mti wa kijani nanyi mkawa kwa huo mnawasha.⁸⁰
81. Kwani aliye ziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye

70 Hii Qur'ani ni kumtia khofu mwenye moyo ulio hai ulio nawirika kwa akili. Na ipite hukumu ya adhabu kuwashukia wanao ipinga Qur'ani, wenye kukataa uwongofu wake.

71 Je! Makafiri wameingiwa na upofu hata hawaoni kwamba Sisi tumewaumbia kutokana na iliyo fanya kudra yetu nyama hoa, wanyama wa mifugo (Ngamia, kondoo, mbuzi na ng'ombe), na wao wamekuwa wanawamiliki, wanawatumilia kama wapendavyo?

72 Na hao wanyama tumewafanya wawatumikie. Wengine basi wanawapanda, na wengine wanawala.

73 Na wanapata kwa hao vitu vya kuwapa manufaa, kama sufi, na manyoya, na nywele, na ngozi, na mafupa, na vinywaji kutokana na maziwa yao. Je! Wanasahau neema hizi hata wamekuwa hawamshukuru aliye waneemesha?

74 Na washirikina wamefanya miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu wakiwaabudu kwa kutaraji kuwa ati watawasaidia.

75 Hiyo miungu ya uwongo haiwezi kuwasaidia kwa lolote Mwenyezi Mungu akiwatakia madhara. Kwani miungu hiyo haiwezi kunafiisha wala kudhuru. Bali wao kwa hiyo miungu isiyo weza kitu, ni kama askari walio tayarishwa kwa ajili ya kuwakhudumia na wa kuwalinda na madhara.

76 Basi yasikuhuzunishe maneno yao kumkhusu Mwenyezi Mungu kwa kumkufuru, na kukukhusu wewe kwa kukwambia mwongo. Hakika Sisi tunayajua wanayo yaficha na wanayo yatangaza. Nasi tutawalipa kwa hayo.

77 Je! Binaadamu anakataa kuwepo Mwenyezi Mungu na uweza wake, na haoni yeye kwamba Sisi, baada ya kuwa hata hayupo, tulimuumba kutokana na tone la manii dhalili? Na sasa amekuwa mkali wa kutukhasimu kwa uwazi kabisa.

78 Tena huyu mpingaji aliye dhaahiri ametupigia mfano ambao kwao anakanya uweza wetu kufufua mafupa baada ya kuoza na kusagika. Na amesahau kuwa Sisi tulimuumba yeye, naye hata hakuwepo aslani. Akasema kwa kukanya na kuona haliwezi kuwa hilo: Ni nani huyo atakaye yafufua mafupa nayo yamekwisha mung'unyika?

79 Ewe Muhammad! Sema: Atayafufua yule yule aliye yaumba hapo mara ya kwanza. Kwani aliye anza anao uweza wa kufanya tena. Naye ni Mkubwa wa kujua kila alichu kiumba. Basi haemewi Yeye na kukusanya vipande vipande baada ya kutawanyika.

80 Aliye kuumbieni moto kutoka mti mbichi, baada ya kwisha kauka. (*Tazama Maelezo 36:80*)

ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi.⁸¹

82. Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.⁸²

83. Basi Ametakasika yule ambaye mkononi mwake umo Ufalme wa kila kitu; na kwake Yeye mtarejeshwa.⁸³

81 Kwani hao wamepotelewa na akili zao hata hawajui kwamba aliye ziumba mbingu na ardhi, juu ya ukubwa wao, ni Muweza vile vile kurejesha kuwaumba wanaadamu ambao ni wadogo na hali yao ni dhaifu? Kwani? Yeye ni Muweza sana, na Yeye ni Mwingi wa kuumba, ambaye ujuzi wake umeenea kila kitu.

82 Hakika shani yake katika kuumba anapo taka kiwe kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Kikawa, na hutokea hapo hapo.

83 Basi Mtukufu ametakasika na kila kisicho laiki na dhati yake, yule ambaye katika kudra yake upo Ufalme wa kila kitu, kwa kuumba, na kupanga, na kuendesha - Kwake Yeye peke yake mtarejeshwa, akuhisabuni kwa a'mali zenu.

Sura 37 - Ass'afat

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kiapo kwa mataifa miongoni mwa viumbe vya Mwenyezi Mungu ambayo yana sifa ya kujipanga kwa safu, na kuzuia, na kusoma. Kiapo hicho ni kuwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mmoja. Na Ishara zinashuhudia kwa hayo. Kwani Yeye ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilio baina yao, na Yeye ni Mola Mlezi wa mashariki na magharibi, ambaye aliye ipamba mbingu ya dunia kwa nyota, na akaifanya ihifadhike na muasi aliye acha ut'iifu wa Mwenyezi Mungu. Na baada ya kuthibitisha itikadi ya Tawhidi, Sura imeendelea kuthibitisha itikadi ya kufufuliwa. Na ikawahadharisha wenye kutia shaka kuwa huko kufufuliwa kutawazukia ghafla nao wanaona. Na ikazileta dalili za kumkinika huko, bali wepesi wa kutokea kwake, na hali wao wanayaona hayo na wanasema: Hii ndiyo Siku ya Hisabu! Na wataambiwa: Hii ndiyo Siku ya mpambanuo mlio kuwa mkiikanusha. Na watakusanywa madhaalimu na walivyo kuwa wakiviabudu. Na watasailiwa na watahojiwa. Na watakuwa wakisingiziana wao kwa wao madhambi walio yapata, na hali wote watakuwa wanashirikiana pamoja katika adhabu. Kwani walijivuna wakakataa kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja, na wakamsingizia Mtume wao kuwa ana kichaa na wazimu; na hali kuwa hapana shaka kuwa kawajia na Haki. Na Mitume wamesema kweli katika waliyo kuja nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na Waumini wenye ikhlasi watastareheshwa kwa kila namna ya neema. Na watazikumbuka neema za Mwenyezi Mungu. Watawatokea watu waovu, na watawaona katikati ya Moto wa Jahim. Watamhimidi Mwenyezi Mungu kwa alivyo walinda, na walivyo okoka wasifuate wito wa wale waovu. Baada ya hayo Sura ikaingia ikieleza mashukio ya walio dhulumu na mashukio ya Waumini. Tena ikafuatiliza kwa kueleza khabari za Mitume wengine ili kumpoza Mtume wa Mwenyezi Mungu, na kuwapa mawaidha watu wake wanao pinga. Na baada ya hadithi mbali mbali za zama mbali mbali na watu mbali mbali, zilizo eleza cheo cha Ujumbe na Wajumbe wenyewe, Sura imetengua madai ya washirikina kwamba Mwenyezi Mungu ana mabinti na wao wana watoto wanaume. Na kwamba Yeye amewafanya Malaika ni wanawake. Na kwamba ipo nasaba ya kukhusiana baina yake na majini. Mwenyezi Mungu Ametakasika na hayo wanayo yazua. Na waja wake ndio watanusuriwa, na jeshi lake ndilo litakalo shinda. Na adhabu yake itaifanya ovu asubuhi ya wanao onywa. Na Sura ikakhitimisha kwa kumtakasa Mola Mlezi wa Utukufu na hayo wanayo mzulia. Na amani ishuke kwa Mitume wote, na Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa wanao jipanga kwa safu.¹
2. Na kwa wenye kukataza mabaya.²
3. Na kwa wenye kusoma Ukumbusho.³
4. Hakika Mungu wenu bila ya shaka ni Mmoja.⁴
5. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, na yaliyomo kati yao, na ni Mola Mlezi wa mashariki zote.⁵
6. Hakika Sisi tumeipamba mbingu ya karibu kwa pambo la nyota.⁶
7. Na kulinda na kila shet'ani a'si.⁷
8. Wasiweze kuwasikiliza viumbe watukufu. Na wanafukuzwa huko kila upande.⁸
9. Wakifurushwa. Na wanayo adhabu ya kudumu.⁹
10. Isipo kuwa anaye nyakua kitu kidogo, na mara humfwatia kimondo kinachong'ara.¹⁰
11. Hebu waulize: Je! Wao ni wenye umbo gumu zaidi au hao wengine tulio waumba. Hakika Sisi tuliwaumba wao kwa udongo unao nata.¹¹
12. Bali unastaajabu, na wao wanafanya maskhara.¹²
13. Na wanapo kumbushwa hawakumbuki.¹³
14. Na wanapo ona Ishara, wanafanya maskhara.¹⁴

1 Naapa kwa mataifa katika viumbe vyangu, walio jipanga wenyewe kwa safu zililo sawa katika msimamo wa ibada na ut'iifu.

2 Na kwa wanao zuia wanao pindukia mipaka kwa mzuio mkali, nidhamu ibakie, na ulimwengu uhifadhiwe.

3 Na kwa wenye kusoma Aya, na wanamdhukuru Mwenyezi Mungu kwa dhikri ya Tasbihi, Kumtakasa, na Kumhimidi, kumsifu.

4 Hakika Mungu wenu anaye faa kuabudiwa bila ya shaka ni Mmoja tu. Hana mshirika wake, kwa dhati, wala kitendo, wala sifa.

5 Yeye - peke yake - ndiye Muumba mbingu na ardhi na viliomo baina yao, na ndiye Mwenye kupanga mambo, na ndiye Mwenye kutawala mashariki za kila chenye mashariki. (*Tazama Maelezo 37:5*)

6 Sisi tumeipamba hii mbingu ya karibu na watu wa duniani kwa mapambo, nayo ni hizo nyota zinazong'ara, zenye ukubwa mbali mbali, na mwahala pao mbali kwenye anga la ulimwengu kama ionekanavyo kwa macho.

7 Na tukaihifadhi hiyo mbingu na kila shetani jabari aliye a'si.

8 Hao majabari wa kishetani hawawezi kusikiliza yanayo pita katika ulimwengu wa Malaika. Na wao hupopolewa kwa kila kinacho faa cha kuwazuia.

9 Hufukuzwa hao kwa nguvu wasifikilie kuweza kusikiliza khabari za mbinguni. Na Akhera watapata adhabu kali ya kudumu.

10 Isipo kuwa anaye lipata neno moja hivi katika khabari za mbinguni kwa kuibia. Na huyo naye tunamwandama kwa mwenge wa moto unao murika anga kwa mwangaza wake, ukamuunguzilia mbali.

11 Ewe Nabii! Hebu waulize hao wanao kanya kufufuliwa wanao ona hayawi hayo: Je! Kwani kuwaumba wao hawa ni kugumu zaidi au kuziumba mbingu, na ardhi, na nyota, na vyenginevyo, tulivyo viumba Sisi?

12 Hakika Sisi tumewaumba wao kutokana na udongo unao gandana. Basi kwa nini wanaona ajabu kurejezwa tena wao?

13 Na wanapo kabiliwa kwa dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu kufufua, hata hawazishughulikia wakanufaika kwa hizo dalili.

14 Na wanapo ona ushahidi wa kuonyesha uweza wa Mwenyezi Mungu huitana wapate kupita mipaka katika kumkejeli.

15. Na husema: Haya si chochote ila ni uchawi tu ulio dhaahiri.¹⁵
16. Ati tukisha kufa na tukawa udongo na mifupa ndio kweli tutafufuliwa?¹⁶
17. Hata baba zetu wa zamani?¹⁷
18. Sema: Naam! Hali nanyi ni madhalili.¹⁸
19. Huko utapigwa ukelele mmoja tu! Na hapo ndio wataona!¹⁹
20. Watasema: Ole wetu! Hii ndiyo Siku ya Malipo.²⁰
21. Hii ndiyo Siku ya Hukumu mliyo kuwa mkiikadhibisha.²¹
22. Wakusanyeni walio dhulumu, na wake zao, na hao walio kuwa wakiwaabudu -²²
23. Badala ya Mwenyezi Mungu. Waongozeni njia ya Jahannamu!²³
24. Na wasimamisheni. Hakika hao watasailiwa:²⁴
25. Mna nini? Mbona hamsaidiani?²⁵
26. Bali hii leo, watasalimu amri.²⁶
27. Watakabiliana wao kwa wao kuulizana.²⁷
28. Watasema: Kwa hakika nyinyi mlikuwa mkitujia upande wa kulia.²⁸
29. Watasema (wakubwa): Bali nyinyi wenyewe hamkuwa Waumini.²⁹
30. Sisi hatukuwa na mamlaka juu yenu, bali nyinyi wenyewe mlikuwa wapotovu.³⁰
31. Basi hukumu ya Mola wetu Mlezi imekwisha tuthibitikia. Hakika bila ya shaka tutaonja tu adhabu.³¹
32. Tulikupotezeni kwa sababu sisi wenyewe tulikuwa wapotovu.³²
33. Basi wao kwa hakika siku hiyo watashirikiana katika adhabu pamoja.³³

15 Na makafiri husema juu ya Ishara zinazo onyesha uweza wa Mwenyezi Mungu: Haya tunayo yaona si chochote ila ni uchawi tu.

16 Hivyo sisi tukisha kufa tukawa udongo na mafupa tutatolewa tena makaburini kwetu tuwe wahai?

17 Sisi tuwe wahai, na pia watafufuliwa baba zetu wa zamani walio kufa kabla yetu, na wakapotea, na wakateketea?

18 Ewe Nabii! Waambie: Ndio mtafufuliwa nyote, nanyi ni madhalili na wanyonge.

19 Kwani hakika kufufuliwa ni Ukelele mmoja tu, mara wote watakuwa wahai wakiyaona waliyo ahidiwa.

20 Na washirikina watasema: Ee msiba wetu huu! Hii ndiyo Siku ya Hisabu na Malipo kwa a'mali zililo tendwa.

21 Watajibiwa: Hii ndiyo Siku ya Hukumu na kufarikisha vitendo, mliyo kuwa mkiikadhibisha.

22 Enyi Malaika wangu! Wakusanyeni walio jidhulumu nafsi zao kwa kufuru, pamoja na wake zao wa kikafiri, na miungu yao waliyo kuwa wakiabudu badala ya Mwenyezi Mungu, yakiwa masanamu au watu, na waonyesheni njia ya kwendea Motoni waingie humo.

23 Tazama tanbihi ya 22.

24 Na wazuieni hapo hapo; kwani wao hakika watahojiwa juu ya imani zao na vitendo vyao.

25 . Enyi washirikina! Mna nini? Mbona hamsaidiani kama mlivyo kuwa mkisaidiana nyinyi kwa nyinyi duniani?

26 Leo hii hawasaidiani, bali leo wanaongozwa tu, wamekwisha salimu amri.

27 Watakuwa wakikabiliana kulaumiana na kusutana, na wakiulizana khabari za mwisho wao muovu.

28 Wanyonge watawaambia walio jipa ukubwa: Nyinyi mlikuwa mkitujia upande tulio udhania ni wa kheri na mafanikio, ili mtugeuze njia tuache Haki twende kwenye upotovu.

29 Watasema walio jipa ukubwa: Sisi hatukukugeuzeni njia, lakini nyinyi wenyewe mliikataa Imani, na mkaipuuza kwa khiari yenu.

30 Na sisi hatukuwa na madaraka juu yenu hata tuweze kukunyang'anyeni uweza wenu wa kukhiari. Bali nyinyi wenyewe mlikuwa watu mlio iacha Haki.

31 Basi neno la Mola wetu Mlezi limethibiti juu yetu. Hakika hapana shaka sisi tutaonja adhabu ya Siku ya Kiyama.

32 Tukakuiteni kwenye maasi na upotovu na nyinyi mkaitikia wito wetu. Kazi yetu ni kufanya hila ya kuwaita watu wafuate upotovu tulio nao. Basi hatuna lawama.

33 Kwani hakika wafuasi na wenye kufuatwa wote watashiriki pamoja katika adhabu ya Siku ya Kiyama.

34. Hivyo ndivyo tutakavyo wafanyia wakosefu.³⁴
35. Wao walipo kuwa wakiambiwa *La ilaha illa 'Llahu* Hapana mungu ila Mwenyezi Mungu tu, wakijivuna.³⁵
36. Na wakisema: Hivyo sisi tuiache miungu yetu kwa ajili ya huyu mtunga mashairi mwendawazimu?³⁶
37. Bali huyu amekuja kwa Haki, na amewasadikisha Mitume.³⁷
38. Hakika nyinyi bila ya shaka mtaionja adhabu chungu.³⁸
39. Wala hamlipwi ila hayo mliyo kuwa mkiyafanya.³⁹
40. Isipo kuwa waja wa Mwenyezi Mungu walio khitariwa.⁴⁰
41. Hao ndio watakao pata riziki maalumu,⁴¹
42. Matunda, nao watahishimiwa.⁴²
43. Katika Bustani za neema.⁴³
44. Wako juu ya viti wamekabiliana.⁴⁴
45. Wanazungushiwa kikombe chenye kinywaji cha chemchem⁴⁵
46. Kinywaji cheupe, kitamu kwa wanywao.⁴⁶
47. Hakina madhara, wala hakiwaleweshi.⁴⁷
48. Na watakuwa nao wanawake wenye macho ya staha mazuri.⁴⁸
49. Hao wanawake kama mayai yaliyo hifadhika.⁴⁹
50. Waingie kuulizana wenyewe kwa wenyewe.⁵⁰
51. Aseme msemaji mmoja miongoni mwao: Hakika mimi nalikuwa na rafiki⁵¹
52. Aliye kuwa akinambia: Hivyo wewe ni katika wanao sadiki⁵²

34. Hakika mfano wa adhabu hiyo Sisi tunawapa wale walio fanya makosa katika Haki ya Mwenyezi Mungu kwa ushirikina na kutenda maasi.

35 Hakika watu hao walikuwa wakiambiwa: *La ilaha illa 'Llahu*, Hapana mungu ila Mwenyezi Mungu tu, wakakataa kukiri kwa kiburi na majivuno.

36 Na husema: Sisi tuache kuabudu miungu yetu kwa kufuata kauli ya mtunga mashairi aliye zugwa asiye kuwa na akili?

37 . Bali Mtume wao amewaletea Tawhidi, Imani ya Mwenyezi Mungu Mmoja, ambayo ndiyo wito wa Mitume wote, naye akasadikisha kwa hivyo wito wa hao Mitume.

38 Enyi washirikina! Hakika nyinyi hapana shaka mtaionja adhabu kali ya Akhera.

39 Na hamtapata malipo Akhera ila malipo ya vitendo vyenu vya duniani.

40 . Ila waja wangu walio safika; hao hawataionja adhabu kwa sababu wao ni watu wa Imani na ut' iifu.

41 Hawa watu wa ikhlasi watapata Akhera riziki maalumu kwa Mwenyezi Mungu.

42 Matunda ya namna mbali mbali. Nao watastareheshwa na kutukuzwa,

43 Katika Bustani zenye neema.

44 Wakikaa humo juu ya viti wakikabiliana.

45 Watawazungukia watoto na chombo chenye kinywaji kilicho toka kwenye chemchem zisio katika.

46 Kinywaji chenye ni cheupe kinapo changanywa, na kitamu kwa wenye kukinywa.

47 Hakiwaumizi kichwa na kuwaletea ghururi, wala kwa kukinywa hicho haiwapotei akili yao kidogo kidogo, yaani hakileweshi.

48 Na watu hawa wat' iifu walioko Peponi watakuwa nao mahuruleini walio safi, wema, macho yao hayawatazami ila waume zao tu, basi hawayatafuti matamanio maovu, jicho la mwema haliangalii ila mema.

49 Hao wanawake wenye macho ya staha ni kama mayai ya mbuni, yaliyo hifadhiwa na mbawa zake. Basi hayaguswi na mikonu, wala hayapati vumbi.

50 Hao watu wema watakuwa wakiingia kuulizana hali, na walikuwaje duniani?

51 Hapo mmoja wao atasema: Mimi nalikuwa na rafiki katika washirikina, akijadiliana nami katika mambo ya Dini na yaliyo kuja katika Qur'ani.

52 Akisema: Ati wewe ni katika hao wanao sadiki kuwa kupo kufufuliwa na kuhisabiwa na kulipwa baada

53. Ati tukisha kufa tukawa udongo na mafupa, ndio tatalipwa na kuhisabiwa?⁵³
54. Atasema: Je! Nyie mnawaona?⁵⁴
55. Basi atachungulia amwone katikati ya Jahannamu.⁵⁵
56. Atasema: Wallahi! Ulikaribia kunipoteza.⁵⁶
57. Na lau kuwa si neema ya Mola wangu Mlezi bila ya shaka ningeli kuwa miongoni mwa walio hudhurishwa.⁵⁷
58. Je! Sisi hatutakufa,⁵⁸
59. Isipo kuwa kifo chetu cha kwanza? Wala sisi hatutaadhibiwa.⁵⁹
60. Hakika huku bila ya shaka ndiko kufuzu kukubwa.⁶⁰
61. Kwa mfano wa haya nawatende watendao.⁶¹
62. Je! Kukaribishwa hivi si ndio bora, au mti wa Zaqquq?⁶²
63. Hakika Sisi tumeufanya huo kuwa ni mateso kwa walio dhulumu.⁶³
64. Hakika huo ni mti unao toka katikati ya Jahannamu.⁶⁴
65. Mashada ya matunda yake kama kwamba vichwa vya mashet'ani.⁶⁵
66. Basi hakika bila ya shaka hao watayala hayo, na wajaze matumbo.⁶⁶
67. Kisha juu yake wanyweshwe mchanganyo wa maji yamoto yaliyo chemka.⁶⁷
68. Kisha hakika marejeo yao bila ya shaka yatakuwa kwenye Jahannamu.⁶⁸

ya kufa?

53 Ati baada ya kwisha teketea, tukawa udongo na mafupa, tutakuja kuwa hai mara nyengine, tuhisabiwe na tulipwe kwa vitendo tulivyo kwisha vitenda?

54 Muumini awaambie wenzie alio kaa nao: Enyi watu wa Peponi, mnawaona watu wa Motoni nipate kumwona rafiki yangu?

55 Jicho lake lipige duru kuelekea Motoni, na huko amwone sahibu yake wa zamani yuko katikati akiadhibika kwa Moto.

56 Akimwona aseme: Wallahi! Ulikaribia kule duniani kunihilikisha lau ningeli kufuata katika ukafiri wako na maasiya yako!

57 Na lau kuwa si neema ya Mola wangu Mlezi kwa hidaya yake na kuniwezesha kwake nikamuamini Mwenyezi Mungu na kufufuka, basi ningeli kuwa mfano wako wewe katika walio hudhurishwa katika hiyo adhabu.

58 Je! Sisi tutakaa milele tukineemeka katika Pepo, wala hatufi kabisa isipo kuwa kule kufa kwetu mara ya kwanza duniani, na wala hatuadhibiwi baada ya kwisha ingia Peponi?

59 Tazama tanbihi ya 58.

60 Hakika haya aliyu tupa Mwenyezi Mungu katika ukarimu wa Peponi bila ya shaka ndiyo kufuzu kukubwa, na kuvuka kukuu na hiyo adhabu tuliyo kuwa tunatahadhari nayo tangu duniani.

61 Ili wapate ukarimu wa Akhera kama walio bahatika kuupata Waumini, basi nawafanye kazi duniani hao wafanyao kazi, ili wapate kama walio pata wao.

62 Je! Hiyo riziki maalumu iliyo andaliwa kwa sababu ya watu wa Peponi ni bora, au mti wa Zaqquq ulio andaliwa kwa ajili ya watu wa Motoni?

63 Hakika Sisi tumeujaalia mti huu uwe ni mtihani na adhabu ya Akhera kwa ajili ya washirikina.

64 . Hakika huo ni mti ulioko katikati ya Jahannamu, umekulia huko Motoni, na umeumbwa kutokana na huko huko.

65 Matunda yake mabaya kuyatazama, yana sura ya kukirihisha, macho hayapendi kuyatazama, kama vichwa vya mashetani ambavyo kwa hakika watu hawajaviona, lakini mtu humpitikia tu katika dhana jinsi ya ubaya wake.

66 Na wao watakuwa wanakula matunda ya mti huo, na wajaze matumbo yao kwayo. Kwani hawanacho kinginecho cha kukila.

67 Kisha washirikina hao juu ya kula mti wa Zaqquq watapewa maji yaliyo changanywa, yamoto, ya kuwababua nyuso zao, na kukatakata matumbo yao.

68 Tena mwisho wao ni Motoni. Wao watakuwa katika adhabu ya milele. Wataletwa kutoka Motoni waje kula mti wa Zaqquq kisha wanyweshe kinywaji hicho, na tena warejeshwe mahala pao katika Jahannamu.

69. Hakika waliwakuta baba zao wamepotea.⁶⁹
70. Na wao wakafanya haraka kufuata nyayo zao.⁷⁰
71. Na bila ya shaka walikwisha potea kabla yao wengi wa watu wa zamani.⁷¹
72. Na Sisi hakika tuliwapelekea waonyaji.⁷²
73. Basi hebu angalia ulikuwaje mwisho wa walio onywa.⁷³
74. Isipo kuwa waja wa Mwenyezi Mungu walio khitariwa.⁷⁴
75. Na hakika Nuhu alitwita, na Sisi ni bora wa waitikiaji.⁷⁵
76. Na tulimwoko ya yeye na ahali zake kutokana na msiba mkubwa.⁷⁶
77. Na tuliwajaalia dhuriya zake ndio wenye kubakia.⁷⁷
78. Na tukamwachia (sifa njema) kwa walio kuja baadaye.⁷⁸
79. Iwe salama kwa Nuhu ulimwenguni kote!⁷⁹
80. Kwa hakika hivi ndivyo tunavyo walipa wanao fanya mema.⁸⁰
81. Hakika yeye ni katika waja wetu walio amini.⁸¹
82. Kisha tukawazamisha wale wengine.⁸²
83. Na hakika Ibrahim alikuwa katika kundi lake,⁸³
84. Alipo mjia Mola wake Mlezi kwa moyo mzima.⁸⁴
85. Alimwambia baba yake na watu wake: Mnaabudu nini?⁸⁵
86. Kwa kuzua tu mnataka miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu?⁸⁶

69 Wao waliwakuta baba zao wamepotoka, na wao wakafanya haraka kufuata zile zile nyayo za baba zao. Wakawa mbioni kwenda njia yao, wakifuata tu wala hawachungui, kama walio timuliwa na wakihimizwa wende mbio mbio kuwafuata hao baba zao bila ya kupima wala kuzingatia.

70 Tazama tanbihi ya 69.

71 Na hakika walipotea njia ya sawa na njia ya Imani wengi katika mataifa yaliyo kwisha tangulia kabla ya hawa washirikina wa Makka.

72 Na bila ya shaka Sisi tuliyatumia Mitume hayo mataifa yaliyo tangulia ili wawaonye na wawahadharisha na adhabu ya Mwenyezi Mungu, nao wakawakadhibisha.

73 Basi angalia, ewe uliye jaaliwa kuangalia, ulikuwaje mwisho wa walio onywa na Mitume? Bila ya shaka waliteketezwa, wakawa ni mazingatio kwa watu.

74 Lakini walikuwapo Waumini ambao aliwakhitari Mwenyezi Mungu wamuabudu Yeye, ili wapate fadhila za ukarimu wake. Basi hao walizipata thawabu zake, na wakaepukana na adhabu yake.

75 Na hakika Nuhu alitwita alipo kwisha kata tamaa na watu wake, basi na Sisi tukawa ni wabora wa kuitikia wito wake, tulipo muitikia ombi lake, na tukawaangamiza watu wake kwa tofani.

76 Na tukamwoko Nuhu na walio amini pamoja naye, wasizame na kuteketea kwa tofani.

77 Tukawajaalia vizazi vya Nuhu ndio walio bakia katika ardhi baada ya kuteketea watu wake.

78 Na tukamwachilia Nuhu kutajwa kwa wema na watu walio kuja baada yake wakimdhukuru mpaka Siku ya Kiyama.

79 Maamkio ya Salama na Amani kumuamkia Nuhu kutokana na Malaika, na watu, na majini.

80 Hakika Sisi huwalipa walio tenda mema mfano wa haya. Basi aliingia katika Jihadi kulinyanyua Neno letu, na akavumilia maudhi kwa ajili yetu.

81 Hakika yeye ni miongoni mwa waja wetu walio tuamini, na wakatimiza ahadi yetu, na wakaufikisha Ujumbe wetu.

82 Kisha tukawazamisha wengine katika makafiri wa kaumu yake.

83 Na hakika bila ya shaka Ibrahim alikuwa akifuata ile ile njia yake na mwenendo wake katika kuitia Tawhidi, Imani Ya Mwenyezi Mungu Mmoja, na kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja.

84 Alipo mkabili Mola wake Mlezi kwa moyo ulio kuwa nadhifu hauna ushirikina, umemsafia ibada Yeye tu.

85 Alipo chukia kuwa baba yake na watu wake wanaabudu masanamu, akawaambia: Ni nini haya masanamu mnayo yaabudu?

86 Si mnazua uwongo tu ulio wazi kwa haya myatendayo, kwa kuwa mnamuabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu? Na si mnataka kuzua uzushi huu bila ya udhuru wowote ila kupenda kwenu tu?

87. Mnamdhania nini Mola Mlezi wa walimwengu wote?⁸⁷
88. Kisha akapiga jicho kutazama nyota.⁸⁸
89. Akasema: Hakika mimi ni mgonjwa!⁸⁹
90. Nao wakamwacha, wakampa kisogo.⁹⁰
91. Basi akaiendea miungu yao kwa siri, akaiambia: Mbona hamli?⁹¹
92. Mna nini hata hamsemi?⁹²
93. Kisha akaigeukia kuipiga kwa mkono wa kulia.⁹³
94. Basi wakamjia upesi upesi.⁹⁴
95. Akasema: Hivyo mnaviabudu vitu mnavyo vichonga wenyewe?⁹⁵
96. Na hali Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni nyinyi na hivyo mnavyo vifanya!⁹⁶
97. Wakasema: Mjengeeni jengo, na kisha mtupeni motoni humo!⁹⁷
98. Basi walitaka kumfanyia vitimbi, lakini tukawafanya wao ndio wa chini.⁹⁸
99. Na akasema: Hakika mimi nahama, nakwenda kwa Mola wangu Mlezi; Yeye ataniongoa.⁹⁹
100. Ewe Mola wangu Mlezi! Nitunukie aliye miongoni mwa watenda mema.¹⁰⁰
101. Basi tukambashiria mwana aliye mpole.¹⁰¹
102. Basi alipo fika makamo ya kwenda na kurudi pamoja naye, alimwambia: Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeona usingizini kuwa ninakuchinja. Basi angalia wewe, waonaje? Akasema: Ewe baba yangu! Tenda unavyo amrishwa, utanikuta

87 Mnamdhania nini huyo ambaye ndiye Mwenye haki ya kuabudiwa kwa kuwa Yeye ndiye Muumba walimwengu wote, mtapo kutana naye na hali nyinyi mmemfanyia washirika wenginewe katika ibada.

88 Basi akazitupia jicho nyota kuzitazama ili apate kuona dalili ya Muumba ulimwengu. Akazia zinageuka, zinabadilika.

89 Akajikhofia nafsi yake asiwe ana upotovu na maradhi ya itikadi.

90 Watu wake wakamwachilia mbali, na wakapuza maneno yake.

91 Akayaendea kwa haraka yale masanamu kwa kificho, na akayapa chakula ambacho wale washirikina walikiweka mbele yao ili nao wapate baraka yao kwa mujibu wa madai yao. Akasema kwa maskhara na kejeli: Mbona hamli?

92 Mna nini hata mmeshindwa kusema lolote, hata ndio au sio?

93 Akayaingilia yale masanamu kuyapiga kwa mkono wa kulia, kwa kuwa ndio wenye nguvu, akayabomoa.

94 Walipo baini kwamba kuvunjwa miungu yao ni kwa kitendo cha Ibrahim, basi walimkimbilia ili wamtese kwa alivyo watendea miungu yao.

95 Ibrahim akawaambia kwa kuwahizi: Hivyo nyinyi mnaabudu mawe mliyo yachonga nyinyi wenyewe kwa mikono yenu? Akili zenu zimekwenda wapi?

96 Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni, na akayaumba hata hayo masanamu mnayo yaunda kwa mikono yenu. Basi Yeye peke yake ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa.

97 Hoja ilipo wapata wale wanao abudu masanamu, wakaona hawana ila waingie kutumia nguvu; wakaazimia kumchoma moto. Basi waliambizana: Mjengeeni jengo, na mlizaje moto, na mtupeni katikati yake!

98 Kwa haya walikusudia kumteketeza, lakini Mwenyezi Mungu alimwoko na ule moto baada ya wao kwisha mtumbukiza humo. Hadhi yake ikawa juu kwa utukufu ule, na Mwenyezi Mungu akawafanya wao ndio watu wa chini.

99 Ibrahim alipo kata tamaa nao, kuwa hawaamini tena, alisema: Mimi ninahama kwendea pahala alipo niamrisha Mola wangu Mlezi nende. Mola wangu Mlezi atanihidi aniongoze mpaka nifike pahala pa utulivu, penye amani, na nchi nzuri.

100 Ewe Mola wangu Mlezi! Nipe dhuriya walio wema wa vitendo, wasimamie hii kazi ya wito kuwaitia watu kwako Wewe, baada yangu.

101 Malaika wakampa bishara ya kwamba atapata mwana atakaye pambwa kwa akili na upole.

mimi, Inshallah, katika wanao subiri.¹⁰²

103. Basi wote wawili walipo jisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji.¹⁰³

104. Tulimwita: Ewe Ibrahim!¹⁰⁴

105. Umekwisha itimiliza ndoto. Hakika hivi ndivyo tunavyo walipa wanao tenda mema.¹⁰⁵

106. Hakika haya ni majaribio yaliyo dhaahiri.¹⁰⁶

107. Basi tukamtolea fidia kwa dhabihu mtukufu.¹⁰⁷

108. Na tukamwachia (sifa njema) kwa watu walio kuja baadaye.¹⁰⁸

109. Iwe salama kwa Ibrahim!¹⁰⁹

110. Hivi ndivyo tunavyo walipa wanao fanya mema.¹¹⁰

111. Hakika yeye ni katika waja wetu walio amini.¹¹¹

112. Na tukambashiria kuzaliwa Is-haqa, naye ni Nabii miongoni mwa watu wema.¹¹²

113. Na tukambarikia yeye na Is-haqa. Na miongoni mwa dhuriya zao walitokea wema na wenye kudhulumu nafsi zao waziwazi.¹¹³

114. Na kwa hakika tuliwafanyia hisani Musa na Haruni.¹¹⁴

115. Na tukawaokoa wao na watu wao kutokana na dhiki kubwa.¹¹⁵

116. Na tukawanusuru; na wakawa wao ndio wenye kushinda.¹¹⁶

117. Na tukawapa wawili hao Kitabu kinacho bainisha.¹¹⁷

102 Akazaliwa huyo mwana, na alipo kuwa kijana wa kwenda naye baba yake katika kutafuta haja za maisha, Ibrahim alipewa mihani kwa ndoto aliyo iota. Ibrahim akasema: Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeona usingizini ufunuo kutokana na Mwenyezi Mungu ananitaka nikuchinje! Basi wewe tazama unaonaje? Yule mwana mwema alisema: Ewe baba yangu! Tekeleza amri ya Mola wako Mlezi. Utaniona mimi katika wanao subiri, Inshallah!

103 Yule baba na mwanawe walipo iridhia hukumu ya Mwenyezi Mungu, na akamweka juu ya fungu la mchanga na akamlaza juu yake, kipaji chake kikawa juu ya ardhi, akawa tayari kumchinja.

104 Na Mwenyezi Mungu akajua umadhubuti wa Ibrahim na mwanawe katika majaribio, Mwenyezi Mungu alimwita Ibrahim kwa wito wa kirafiki: Ewe Ibrahim! Hakika umeitikia kwa utulivu huo ufunuo wa ndoto, na wala hukusitasita katika kufuata amri. Basi haya yanakutosha. Sisi tunakupunguzia haya majaribio yetu kuwa ni malipo kwa wema wako, kama tunavyo walipa walio wema kwa wema wao.

105 Tazama tanbihi ya 104.

106 Hakika majaribio haya tuliyo mjaribia Ibrahim na mwanawe bila ya shaka ni majaribio yaliyo dhihirisha undani wa Imani yao na yakini yao kwa Mola Mlezi wa walimwengu.

107 Na tukamkomboa kwa mhanga wenye cheo kikubwa, kwa kuwa hayo ni kwa amri ya Mwenyezi Mungu.

108 Na tukaacha atajike kwa sifa nzuri katika ndimi za walio kuja baada yake.

109 Maamkio ya amani na salama kwa Ibrahim!

110 Mfano wa malipo kama haya ya kuwakinga na balaa ndivyo tunavyo walipa walio wema katika kufuata amri za Mwenyezi Mungu.

111 Hakika Ibrahim ni katika waja wetu wanao ifuata Haki.

112 Na kwa amri yetu, Malaika walimbashiria kuwa ataruzukiwa mwana, Is-haqa juu ya kukata tamaa na kuwa mkewe ni tasa. Na kwamba yeye hakika atakuwa Nabii miongoni mwa walio wema.

113 Nasi tukamtunukia yeye na mwanawe baraka na kheri duniani na Akhera. Na miongoni mwa vizazi vyao watatokea watakao jifanyia wema nafsi zao kwa Imani na ut'iifu, na watakao jidhulumu kwa upotovu wa ukafiri na maasi.

114 Na bila ya shaka tuliwaneemesha Musa na Haruni kwa kuwapa Unabii na neema kubwa kubwa.

115 . Na tukawaokoa wao na watu wao kutokana na dhiki kubwa iliyo kuwa iwashukie kutokana na Firauni na kaumu yake.

116 Na Sisi tukawanusuru na adui zao, wakawa wao ndio wenye kushinda.

117 Na tukampa Musa na Haruni Kitabu kilicho wazi chenye kubainisha hukumu za Dini, nacho ni Taurati.

118. Na tukawaongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka.¹¹⁸
119. Na tukawaachia (sifa njema) katika watu walio kuja baadaye.¹¹⁹
120. Iwe salama kwa Musa na Haruni!¹²⁰
121. Hakika hivyo ndivyo tunavyo walipa walio wema.¹²¹
122. Hakika wawili hao ni katika waja wetu walio amini.¹²²
123. Na hakika Ilyas bila ya shaka alikuwa miongoni mwa Mitume.¹²³
124. Alipo waambia watu wake: Hamwogopi?¹²⁴
125. Mnamwomba Baa'li na mnamwacha Mboru wa waumbaji,¹²⁵
126. Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu na Mola Mlezi wa baba zenu wa zamani?¹²⁶
127. Wakamkadhibisha. Basi kwa hakika watahudhurishwa;¹²⁷
128. Isipo kuwa waja wa Mwenyezi Mungu walio safishwa.¹²⁸
129. Na tumemwachia (sifa nzuri) kwa walio kuja baadaye.¹²⁹
130. Iwe salama kwa Ilyas.¹³⁰
131. Hakika hivyo ndivyo tunavyo walipa walio wema.¹³¹
132. Hakika yeye ni katika waja wetu walio amini.¹³²
133. Na hakika Lut'i bila ya shaka ni miongoni mwa Mitume.¹³³
134. Tulipo mwokoza yeye na ahali zake wote,¹³⁴
135. Isipo kuwa mwanamke mkongwe katika wale walio bakia nyuma.¹³⁵
136. Kisha tukawaangamiza wale wengineo.¹³⁶
137. Na hakika nyinyi mnawapitia wakati wa asubuhi,¹³⁷
138. Na usiku. Basi je! Hamyatii akilini?¹³⁸
139. Na hakika Yunus alikuwa miongoni mwa Mitume.¹³⁹

118 Na tukawaongoza waifuata Njia iliyo sawa.

119 Na tukabakisha sifa njema za kutajika wote wawili hao kwa watu wengineo walio kuja baada yao.

120 Maamkio ya Amani na Salama kwa Musa na Haruni.

121. Hakika mfano wa malipo tuliyo mjazi Musa na Haruni ndivyo tunavyo wajazi wote walio wema.

122. Hakika wawili hao ni katika waja wetu wenye kuifuata Haki.

123 Na hakika Ilyas ni katika hao tulio watuma kwenda waongoa watu wao.

124 Ilyas alipo waambia watu wake, nao walikuwa wakiiyaabudu masanamu yao: Je! Mnaendelea juu ya makosa yenu, na wala hamumkhofu Mwenyezi Mungu mkajikinga na adhabu yake?

125 Mnaliabudu sanamu linalo itwa Baa'li, na mkaacha kumuabudu Mwenyezi Mungu aliye uumba ulimwengu na akaufanya mzuri uumbaji wake?

126 Mwenyezi Mungu amekuumbeni na amekuhifadhini nyinyi na baba zenu wa zamani. Yeye basi ndiye Mwenye haki ya kuabudiwa.

127 Lakini walimkadhibisha, basi jaza yao ni kuhudhurishwa kwenye Moto Siku ya Kiyama.

128 Isipo kuwa waja wa Mwenyezi Mungu walio safisha Imani yao. Hao basi ndio wenye kufuzu.

129 Na tukamjaalia awe anatajwa kwa wema na ndimi za walio kuja baada yake.

130 Salamu juu ya Ilyasi, au juu yake yeye na watu wake, kwa kuwa kawashinda.

131 Hakika mfano wa malipo tuliyo mlipa Ilyas tunamlipa kila aliye mwema kwa sababu ya wema wake.

132 Hakika Ilyas ni katika waja wetu walio amini.

133 Na hakika Lut'i ni katika Mitume tulio watuma ili afikishe Ujumbe wetu kwa watu.

134 Kwa hakika Sisi tumemwokoza yeye na ahali zake wote kutokana na adhabu iliyo wasibu watu wake.

135 Ila mkewe mkongwe. Yeye bila ya shaka aliteketea pamoja na walio teketea.

136 Kisha tukawaangamiza wote isipo kuwa Lut'i na walio muamini.

137 Na hakika nyinyi, watu wa Makka, mnayapitia majumba ya hao kaumu Lut'i katika safari zenu za kwendea Sham asubuhi au usiku. Je! Mmpotelewa na akili zenu hata hamwezi kuzingatia yaliyo wapitia hao kuwa ni malipo ya ukanushaji wao?

138 Tazama tanbihi ya 137.

139 Na hakika Yunus ni miongoni mwa tulio watuma wawafikishie Ujumbe wetu watu.

140. Alipo kimbia katika jahazi lilio sheheni.¹⁴⁰
141. Akaingia katika kupigiwa kura, na akawa katika walio shindwa.¹⁴¹
142. Samaki akammeza hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa.¹⁴²
143. Na ingeli kuwa hakuwa katika wanao mtakasa Mwenyezi Mungu,¹⁴³
144. Bila ya shaka angeli kaa ndani yake mpaka siku ya kufufuliwa.¹⁴⁴
145. Lakini tulimtupa ufukweni patupu, hali yu mgonjwa.¹⁴⁵
146. Na tukauotesha juu yake mmea wa kabila ya mung' unye.¹⁴⁶
147. Na tulimtuma kwa watu laki moja au zaidi.¹⁴⁷
148. Basi wakaamini, na tukawastarehesha kwa muda.¹⁴⁸
149. Basi waulize: Ati Mola wako Mlezi ndiye mwenye watoto wa kike, na wao wanao watoto wa kiume?¹⁴⁹
150. Au tumewaumba Malaika kuwa ni wanawake, na wao wakashuhudia?¹⁵⁰
151. Ati ni kwa uzushi wao ndio wanasema.¹⁵¹
152. Mwenyezi Mungu amezaa! Ama hakika bila ya shaka hao ni waongo!¹⁵²
153. Ati amekhiari watoto wa kike kuliko wanaume?¹⁵³
154. Mna nini? Mnahukumu vipi nyinyi?¹⁵⁴
155. Hamkumbuki?¹⁵⁵

140 Alipo wahama watu wake bila ya amri ya Mola wake Mlezi, akaliendea jahazi ambalo lilio kwisha sheheni pomoni, akalipanda. Jahazi likapatikana na mambo ikawajibikia lazima mmoja katika abiria atoswe kupunguza shehena yake. Kura ikamuangukia Yunus, akashindwa kwa kura. Akatoswa baharini kwa mujibu wa ada yao zama zile.

141 Tazama tanbihi ya 140.

142 Samaki akammeza, naye hakika alistahiki lawama kwa kuikimbia kazi yake ya Daa'wa, Wito, kuwaitia watu wafuate Haki, na kuacha kuwasubiria wale walio kwenda kinyume naye..

143 Na lau kuwa Yunus hakuwa katika wanao mtakasa Mwenyezi Mungu, wanao dumu kumdhukuru, angeli kufa ndani ya samaki, wala asingeli toka humo mpaka siku ya kufufuliwa.

144 Tazama tanbihi ya 143.

145 Tukamtupa pahali patupu kwenye nchi pasipo kuwa na miti wala majumba, naye ni mgonjwa kwa yaliyo mpa. (*Tazama Maelezo 37:145*)

146 Tukauotesha mmea wa kutambaa, usio simama juu ya kigogo, ukamfunika na kumkinga na madhara ya hali ya hewa.

147 Hata alipo pata nafuu kutokana na yaliyo msibu, tukamtuma awaendee watu wengi. Wanasema walio waona kuwa wanapata laki moja au zaidi.

148 Wakauwitikia wito wake, nasi tukawakunjulia neema zetu kwa muda maalumu.

149 Ewe Nabii! Waulize watu wako: Ati Mwenyezi Mungu aliye kuumba ana watoto wa kike kinyume na wao; na wao ndio wana watoto wanaume kinyuma na Yeye.

150 Ati tumewaumba Malaika kuwa ni wanawake, na wao hao makafiri waliona kwa macho yao kuumba kwao, na ndio wakasimulia walio yaona.

151 Ewe mwenye kusikia! Yazingatie maneno yao. Hakika wao kwa uwongo wao wanasema: Mwenyezi Mungu amezaa! Na hali Yeye ametakasika na upungufu kama huo wa kuwa mzazi au kuzaliwa. Na hakika bila ya shaka hao ni waongo kwa usemi huo, kwa ushahidi wa dalili nyingi za Upweke wake.

152 Tazama tanbihi ya 151.

153 Ati Yeye amejichagulia mwenyewe mabinti ambao kwa madai yenu ndio mnawachukia kuliko watoto wa kiume ambao mnawapenda, na hali Yeye ndiye Mwenye kuwaumba wote, watoto wa kike na wa kiume.

154 Ni nini lilio kusibuni hata mkakata hukumu bila ya ushahidi? Vipi mnahukumu hivyo na hali ni upotovu ulio wazi.

155 Je! Mmesahau dalili za uweza wake na kutakasika kwake, ndio msikumbuke mpaka mkaingia katika upotovu.

156. Au mnayo hoja iliyo wazi?¹⁵⁶
157. Basi leteni Kitabu chenu kama mnasema kweli.¹⁵⁷
158. Na wameweka makhusiano ya nasaba baina yake na majini; na majini wamekwisha jua bila ya shaka kuwa wao watahudhurishwa.¹⁵⁸
159. *Subhana 'Llah* Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayo msingizia.¹⁵⁹
160. Isipo kuwa waja wa Mwenyezi Mungu walio safishwa.¹⁶⁰
161. Basi hakika nyinyi na mnao waabudu¹⁶¹
162. Hamwezi kuwapoteza¹⁶²
163. Isipo kuwa yule atakaye ingia Motoni.¹⁶³
164. Na hapana katika sisi ila anapo mahali pake maalumu.¹⁶⁴
165. Na hakika bila ya shaka sisi ndio wajipangao safu.¹⁶⁵
166. Na hakika sisi ndio wenye *kusabihi* kutakasa.¹⁶⁶
167. Na walikuwapo walio kuwa wakisema:¹⁶⁷
168. Tungeli kuwa na Ukumbusho kama wa watu wa zamani,¹⁶⁸
169. Bila ya shaka tungeli kuwa ni waja wa Mwenyezi Mungu wenye ikhlasi.¹⁶⁹
170. Lakini waliukataa. Basi watakuja jua.¹⁷⁰
171. Na bila ya shaka neno letu lilikwisha tangulia kwa waja wetu walio tumwa.¹⁷¹
172. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakao nusuriwa.¹⁷²
173. Na kwamba jeshi letu ndilo litakalo shinda.¹⁷³

156 Hebu nyinyi mnazo nguvu za ushahidi wa kubainisha wa kuthibitisha hayo mnayo yadai?

157 Basi leteni hoja zenu, ikiwa mnazo hoja za katika Kitabu cha mbinguni, kama nyinyi ni wakweli katika hayo myasemayo na mnayo yahukumia.

158 Wakashikilia katika itikadi zao, na wakazua baina ya Mwenyezi Mungu na majini, ambao hawawaoni, kuwa ati yapo makhusiano ya nasaba. Na bila ya shaka hao majini walikwisha jua kuwa makafiri watahudhurishwa mbele ya Mwenyezi Mungu ili wapate malipo yao yasiyo kimbilika.

159 Mwenyezi Mungu Mtukufu ametakasika na hizo sifa za kuemewa na za upungufu wanazo mzulia kuwa anazo.

160 Lakini waja wa Mwenyezi Mungu walio khitariwa wakasafishwa hawana makosa ya huo uzushi wa makafiri.

161 Enyi makafiri! Hakika nyinyi, na hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu - Nyinyi kwa kuwaabudu kwenu badala yake Yeye, hamtampoteza yeyote kwa upotovu wenu. Isipo kuwa yule ambaye tangu hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anamjua ni katika watu wa Motoni, na huko ataingia.

162 Tazama tanbihi ya 161.

163 Tazama tanbihi ya 161

164 Na Malaika kuwania kuwa wao ni waja wa Mwenyezi Mungu, wakasema: Hapana yeyote katika sisi ila ana cheo chake maalumu katika ujuzi, na ibada, na wala hakikiuki hicho.

165 Na sisi tumejipanga safu wenyewe katika misimamo ya kutumika daima.

166 Na hakika sisi bila ya shaka yoyote ndio wenye kumtakasa Mwenyezi Mungu na kila lisilo kuwa na maelekeo naye katika kila hali.

167 Na walikuwapo makafiri wa Makka kabla ya kuteuliwa Mtume s.a.w. ambao wakisema: Lau kuwa sisi tungeli kuwa na Kitabu kama Vitabu vya watu wa zamani, yaani kama Taurati na Injili, nasi bila ya shaka tungeli kuwa waja wa Mwenyezi Mungu wenye kumsafia ibada Yeye.

168 Tazama tanbihi ya 167.

169 Tazama tanbihi ya 167.

170 Na Kitabu kikawajia, nao wakakikataa. Basi watakuja jua nini matokeo ya kukataa kwao.

171 Ninaapa! Hukumu yetu kwa Mitume tulio watuma imekwisha tolewa mbele, ya kwamba ushindi na matokeo mema ni yao wao dhidi ya makafiri.

172 Tazama tanbihi ya 171.

173 Na kwamba wafuasi wetu na wasaidizi wetu ndio peke yao watakao washinda walio kengeuka.

174. Basi waachilie mbali kwa muda.¹⁷⁴
175. Na watazame, nao wataona.¹⁷⁵
176. Je! Wanaihimiza adhabu yetu?¹⁷⁶
177. Basi itakapo shuka uwanjani kwao, itakuwa asubuhi mbaya kwa walio onywa.¹⁷⁷
178. Na waache kwa muda.¹⁷⁸
179. Na tazama, na wao wataona.¹⁷⁹
180. *Subhana Rabbi'l'Izzat* Ametakasika Mola Mlezi Mwenye enzi na yale wanayo mzulia.¹⁸⁰
181. Na Salamu juu ya Mitume.¹⁸¹
182. Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹⁸²

174 Basi waachilie mbali, nawe ngoja mpaka wakati ujao. Kwani Sisi tutakupa wewe matokeo mema, na manusura, na ushindi.

175 Nawe watazame, na uangalie vyema adhabu gani na mateso yatakayo wapata kwa kwenda kinyume nawe na kukukadhibisha. Basi watakuja ona kwa macho yao zitakavyo shindwa safu zao, na wataona nusura ya Mwenyezi Mungu inavyo wafikia Waumini.

176 Je! Wamepoteza akili zao nini, hata wakawa wanaihimiza adhabu yetu?

177 Basi adhabu hiyo itakapo teremka kwenye uwanja wao mpana, itakuwa asubuhi oву kweli hiyo kwa hao walio onywa na adhabu.

178 Na waachilie mbali mpaka mambo yatakapo waishia.

179 Na yaangalie yatakayo wafika wao na yatakayo kufika wewe. Wao watakuja yaona hayo wanayo yahimiza.

180 Mwenyezi Mungu, aliye kuumba wewe na aliye ziumba nguvu na ushindi, ametakasika na huo uzushi wanao muambatisha naye.

181 Na salamu zishuke juu ya Mitume wapenzi walio safika.

182 Na sifa njema ni za Mwenyezi Mungu peke yake, Muumba wa viumbe vyote, na Mwenye kuwaangalia makhaluku wote.

Sura 38 - S'aad

Utangulizi

Sura hii ni ya thalathini na nane katika Sura za Qur'ani Tukufu. Nayo ni Sura ya Makka, na Aya zake ni 88.

Sura hii inatueleza namna ya inda ya washirikina waliyo kuwa wakiufanyia Wito wa Nabii Muhammad s.a.w. na uhasidi wao kwa vile Mwenyezi Mungu alivyo mkirimu kwa kumpa utukufu wa Utume, na kumteremshia Qur'ani. Basi inawajibu kwa yale mawazo ya uwongo walio mnasibishia nayo. Na imebainisha kwamba yaliyo wapelekea kuupiga vita Wito wake kama wafanyavyo si lolote ila ni dharau ya uwongo, na kupenda kuleta khitilafu na mgawanyo. Na lau kuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu inge wateremkia, msimamo wao kwa Mtume s.a.w. usingeli kuwa hivyo ulivyo. Kisha Mwenyezi Mungu amewapigia mifano ya kaumu zilizo kwisha tangulia, ili wapate kuacha inadi na kuleta dhiki, na ili kumpa moyo Mtume wake s.a.w. kufikisha Wito, na hata ange pata taabu zozote na vitimbi vyovyote vya washirikina kwa ajili yake. Na apate kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema alizo mpa, kama walivyo fanya ndugu zake Manabii na Mitume wengine. Na kutokea na haya anataja marejeo mema aliyo waandalia Mwenyezi Mungu wachamngu, na maangukio maovu aliyo waandalia wenye kuasi. Kisha akawakumbusha yaliyo kuwa baina ya baba yao Adam a.s. na adui yake Iblisi, ili wajue kuwa anayo waitia Iblisi kufanya kiburi kwa kupinga kufwata haki ni tabia katika tabia zake Iblisi. Na kupanda kiburi huku ndiko kulikuwa sababu ya kufukuzwa kwake kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu.

Sura imekhitimisha kwa kueleza vilivyo kazi muhimu ya Mtume s.a.w., nayo ni kufikisha Wito, na kwamba yeye hawataki ujira kwa hayo, na yeye hakujileta nafsi yake. Na Qur'ani si chochote ila ni Ukumbusho kwa walimwengu wote. Na bila ya shaka watakuja jua ukweli wa khabari zake baadae

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. S'ad, Naapa kwa Qur'ani yenye mawaidha.¹
2. Lakini walio kufuru wamo katika majivuno na upinzani²
3. Mataifa mangapi tumeyaangamiza kabla yao, na wakapiga kelele, lakini wakati wa kuokoka ulikwisha pita.³
4. Na walistaajabu kuwajia mwonyaji anaye tokana nao wenyewe, na makafiri wakasema: Huyu ni mchawi, mwongo.⁴

1 S'ad: Ni harufi iliyo anzia Sura hii kama zilivyo anzia baadhi ya Sura nyengine kwa mpango wa Qur'ani katika kuanzia kwa harufi moja moja. Naapa kwa Qur'ani yenye utukufu na shani kubwa kuwa hakika hii ni Kweli isiyoyote.

2 Lakini walio kufuru wamo katika majivuno, hawataki kufuata Haki, na wanawafanyia inda watu wa Haki.

3 Mataifa mengi tuliyateketeza kabla yao, wakapiga kelele kutaka msaada ilipo wafikia adhabu. Lakini huo haukuwa wakati wa kuiepuka adhabu.

4 Na walistaajabu watu hawa kuwa amewajia Mtume binaadamu kama wao, na wakasema hao wanao

5. Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu.⁵
6. Na wakaondoka wakubwa wao wakiwaambia: Nendeni zenu na dumuni na miungu yenu, kwani hili ni jambo lililo pangwa.⁶
7. Sisi hatukusikia haya katika mila hii ya mwisho. Haya si chochote ila ni uzushi tu.⁷
8. Ati yeye tu ndiye aliye teremshiwa mawaidha peke yake katika sisi? Lakini hao wana shaka na mawaidha yangu, bali hawajaionja adhabu yangu.⁸
9. Au wanazo wao khazina za rehema za Mola wako Mlezi, Mwenye nguvu, Mpaji?⁹
10. Au wao wana ufalme wa mbingu na ardhi na viliomo kati yao? Basi nawazipande njia za kwendea huko!¹⁰
11. Hao ni askari watao shindwa miongoni mwa makundi yatayo shindwa.¹¹
12. Walikanusha kabla yao kaumu ya Nuhu, na kina A'adi na Firauni mwenye majengo.¹²
13. Na Thamud na kaumu Lut'i na watu wa Machakani. Hayo ndiyo makundi.¹³
14. Hao wote waliwakadhibisha Mitume; basi wakastahiki adhabu yangu.¹⁴
15. Na hawa hawangojei ila ukelele mmoja tu usio na muda.¹⁵
16. Na wao husema: Mola wetu Mlezi! Tuletee upesi sehemu yetu ya adhabu kabla ya Siku ya Hisabu.¹⁶
17. Subiri kwa hayo wayasemayo, na umkumbuke mja wetu Daudi, mwenye nguvu. Hakika yeye alikuwa mwingi wa kutubia.¹⁷

upinga Ujumbe wake: Huyu ni mdanganyifu, mwongo.

5 Ati amewafanya miungu yote kuwa ni Mungu mmoja tu! Ama hakika jambo hili ni la ajabu, mwisho wa kustajabisha.

6 Wakubwa wao wakakimbilia kuusiana wao kwa wao wakiambiana: Endeleeni na njia yenu hiyo hiyo, na shikilieni kuiabudu miungu yenu. Kwani hakika tumepangiwa jambo kubwa hili.

7 Hatujapata kusikia haya mambo ya Tawhidi, kumfanya Mungu mmoja tu, katika dini ya baba zetu tulio wawahi kuwaona. Haya si chochote ila ni uwongo tu ulio zuliwa.

8 Basi katika sote sisi, amechaguliwa Muhammad tu peke yake kupewa hishima ya kuteremshiwa Qur'ani.

9 Bali sisi tunawauliza hawa wanao kuhusudu: Kwani wao wanazo khazina za rehema ya Mola wako Mlezi Mwenye nguvu, Mwingi wa kutoa, hata wao wawe ndio wa kuteua nani wa kumpa Unabii kwa mujibu wa mapenzi ya nafsi zao?

10 Tena tunawauliza: Kwani wao wanao ufalme wa mbingu na ardhi na viliomo baina yao? Ikiwa hivyo basi nawazipande ngazi mpaka wafikie pahala ambapo watakuwa wakitoa hukumu kama watakavyo, kama wanaweza!

11 Hao ni askari wanyonge walio shindwa, hapana hivi wala hivi, kama walivyo shindwa mfano kama wao walio jikusanya kuwapinga Manabii.

12 Kabla ya hawa, walikadhibisha kaumu ya Nuhu, kina A'adi na Firauni aliye kuwa na majengo makubwa yaliyo simama imara kama milima, na kina Thamudi na Kaumu Lut'i na Kaumu ya Shu'ayb, na watu wa Machakani, kwenye miti mingi iliyo shikamana. Hao ndio walio jumuika kuwapinga Mitume wao kama walivyo jumuika watu wako.

13 Tazama tanbihi ya 12.

14 Hapana mmoja katika hao wote ila alimkadhibisha Mtume wake, na kwa hivyo ikawashukia adhabu yangu.

15 Na hao walio jiunga kuwapinga Mitume hawangojei ila ukelele mmoja usio hitajia kukaririwa.

16 Na makafiri husema kwa kejeli: Mola wetu Mlezi! Tuhimizie sehemu yetu ya adhabu kabla ya Siku ya Malipo

17 Ewe Muhammad! Yastahamilie hayo wanayo yasema juu yako washirikina. Na mkumbuke mja wetu, Daudi, mwenye nguvu katika Dini na dunia. Hakika yeye alikuwa mwingi wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu katika hali zote.

18. Hakika tuliidhalilisha milima pamoja naye ikisabihi jioni na asubuhi pamoja naye.¹⁸
19. Napia ndege walio kusanywa makundi kwa makundi; wote walikuwa wanyenyekevu kwake.¹⁹
20. Na tukautia nguvu ufalme wake, na tukampa hikima, na kukata hukumu.²⁰
21. Na je! Imekufikia khabari ya wagombanao walipo pindukia ukuta kuingia chumbani?²¹
22. Walipo muingilia Daudi, naye akawaogopa. Wakasema: Usiogope! Sisi ni wagombanao wawili, mmoja wetu amemdhulumu mwenziwe. Basi tuhukumu kwa haki, wala usipendele. Na utuongoe kwenye njia iliyo sawa.²²
23. Hakika huyu ndugu yangu ana kondoo wa kike tisiini na tisa; na mimi ninaye kondoo mke mmoja. Akasema: Nipe huyo nikufugie! Na amenishinda kwa maneno.²³
24. Akasema: Kweli amekudhulumu kwa kumtaka kondoo wako mmoja kuongezea kwenye kondoo wake. Na hakika washirika wengi hudhulumiana wao kwa wao, isipo kuwa walio amini na wakatenda mema. Na hao ni wachache. Na Daudi akajua kuwa tumemfanyia mtihani. Basi akamwomba msamaha Mola wake Mlezi, na akaanguka kusujudu na kutubia.²⁴
25. Basi tukamsamehe kwa hayo. Naye kwa hakika anao mkaribisho mkubwa na marejeo mazuri kwetu.²⁵
26. Ewe Daudi! Hakika Sisi tumekufanya wewe uwe Khalifa katika nchi. Basi wahukumu watu kwa haki, wala usifuate matamaniao yakakupoteza kwenye Njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika wanao ipotea Njia ya Mwenyezi Mungu wakaiacha, watapata adhabu kali kwa sababu ya kusahau kwao Siku ya Hisabu.²⁶

18 Hakika Sisi tuliidhalilisha milima pamoja naye, yeye akichuma manufaa kutoka humo, na hiyo milima ikimtakasa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kila upungufu, wakati wa mwisho wa mchana na mwanzo wake.

19 Na pia tukamdhalilishia ndege walio kusanywa kutokana na kila namna na kila pahali. Vyote hivyo, milima na ndege, vikimwitikia Daudi kama atakavyo, akivisarifu kama apendavyo kwa maslahi ya umma.

20 Tukautia nguvu ufalme wake, na tukampa Unabii na kupambanua baina ya Haki na baat'ili.

21 Ewe Muhammad! Ati imekujia khabari ya makhasimu wagombanao, walio mjia Daudi kwa kupindukia kuta za mihrabuni palipo kuwa pahala pake pa ibada? Hawakupita mlangoni.

22 Walipo muingilia Daudi, naye akawaogopa, akababaika. Wakasema: Usikhofu kitu. Sisi ni wenye kuzozana, tumedhulumiana. Basi tuhukumu kwa uadilifu wala usiupindukie huo uadilifu. Na tuongoze kwenye njia iliyo sawa sawa.

23 Mmoja wa hao wagombanao alisema: Hakika huyu ndugu yangu anao kondoo wa kike tisiini na tisa, na mimi ninaye kondoo mmoja tu. Akasema: Nache niwe nakuchungia kama ninavyo wachunga wangu. Na akanishinda katika usemi.

24 Daudi akasema kabla hajasikia maneno ya yule mwenye ugomvi mwengine: Hakika huyu amekudhulumu kwa kumtaka kondoo wako amchanganye na wale wake. Na hakika wengi wenye kushirikiana hudhulumiana wao kwa wao, isipo kuwa wale ambao Imani yao imetulia katika nyoyo zao, na wakawa wanatenda mema. Na watu kama hao ni wachache, shida kupatikana. Na Daudi akajua kuwa jambo hili si chochote ila ni mtihani tuliyo mfanyia Sisi. Basi akaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, na akainama kurukuu kwa Mwenyezi Mungu, na akarejea kwa Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu.

25 Na Sisi tukamsamehe kule kufanya haraka ya kutoa hukumu. Na hali yeye ana hadhi na marejeo mazuri kwetu.

26 Na Mwenyezi Mungu alimfunulia kwa kumwambia: Ewe Daudi! Hakika Sisi tumekufanya wewe uwe Khalifa, yaani Naibu, wetu katika ardhi. Basi wahukumu watu kwa sharia niliyo kupa, wala usiendeshe hukumu kufuata matamaniao yao, yakakupotosha njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika wendao pogo na njia ya Mwenyezi Mungu kwa kufuata matamaniao yao wao watapata adhabu kali kwa kughafilika kwao na Siku ya Malipo.

27. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya walio kufuru. Ole wao walio kufuru kwa Moto utao wapata.²⁷
28. Je! Tuwafanye walio amini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au tuwafanye wachamngu kama waovu?²⁸
29. Na hiki Kitabu, tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya zake, na wawaidhike wenye akili.²⁹
30. Na Daudi tukamtunukia Suleiman. Alikuwa mja mwema. Na hakika alikuwa mwingi wa kutubia.³⁰
31. Alipo pelekewa jioni farasi wasimamao kidete, tayari kutoka shoti;³¹
32. Basi akasema: Navipenda vitu vizuri kwa kumkumbuka Mola wangu Mlezi. Kisha wakafichikana nyuma ya boma.³²
33. (Akasema:) Nirudishieni! Akaanza kuwapapasa miguu na shingo.³³
34. Na tulimtia mtihani Suleiman, na tukauweka mwili juu ya kiti chake, kisha akarejea kwa kutubu.³⁴
35. Akasema: Mola wangu Mlezi! Nisamehe na unipe ufalme usio mwelekea yeyote baada yangu. Hakika Wewe ndiye Mpaji.³⁵
36. Basi tukaufanya upepo umtumikie, ukenda kwa amri yake, popote alipo taka kufika.³⁶
37. Na tukayafanya mashet'ani yamtumikie, wote wajenzi na wapiga mbizi.³⁷
38. Na wengine wafungwao kwa minyororo.³⁸

27 Wala Sisi hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo baina yao kwa mchezo. Hayo ndiyo wanayo yadhania makafiri. Na kwa hivyo wakapitisha hukumu kwa mujibu wa pumbao zao. Basi hao walio kufuru watapata adhabu kali ya Moto.

28 Inaelekeana vipi na hikima yetu na uadilifu wetu tuwafanye sawa baina ya Waumini wenye kutenda mema, na wale wanao fanya uharibifu katika ardhi? Au yaeleke vipi tuwaweke sawa baina ya wenye kuikhofu adhabu yetu na wakaiogopa ikabu yetu na wale walio waasi wakenda kinyume na hukumu zetu?

29 Ewe Muhammad! Hichi tulicho kuteremshia ni Kitabu chenye manufaa mengi, ili wenye akili nzuri na nyoyo za kufahamu wapate kuzielewa Aya zake, na wawaidhike kwazo.

30 Na Daudi tulimtunukia mwana, aitwaye Suleiman, mwenye kustahiki sifa nzuri, ambaye anafaa kuitwa, "Mja mwema kweli". Kwa sababu yeye alikuwa mwingi mno wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu katika kila hali.

31 Na hebu taja katika khabari za Suleiman kuwa alipelekewa alasiri farasi wa asli ambao hutulia wanapo simama, na huenda mbio wanapo kwenda.

32 Suleiman akasema: Hakika mimi nimenyweshwa mapenzi ya farasi, kwa sababu hawa ni katika matayarisho ya mambo ya kheri, nayo ni Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Mapenzi haya yametokana na kumkumbuka Mola wangu Mlezi. Na hakisita kushughulika kuwaangalia mpaka wakapotea machoni mwake.

33 Akaamrisha warudishwe tena kwake apate kujua hali yao. Akaingia kuwapapasa miundi ya miguu yao na shingo zao kwa upole na mapenzi juu yao.

34 Na hakika Sisi tulimfanyia mtihani Suleiman ili asighurike na heba ya ufalme. Tukaweka juu ya kiti chake kiwiliwili kisicho weza kuendesha mambo. Akautambua mtihani, akarejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na akatubu.

35 Suleiman alimwomba Mola wake Mlezi kwa kurejea kwake: Mola wangu Mlezi! Nighufirie yaliyo toka kwangu kwa ghafla, na unitunukie ufalme usio elekea yeyote kuupata baada yangu. Hakika Wewe ndiye Mwingi wa kutunukia, na ndiye Mwingi wa kutoa.

36 Tukamdhalilishia upepo, ukenda kama anavyo taka maridhawa, kokote aliko kusudia na kutaka.

37 Na tukamdhalilishia kila mjenzi na mpiga mbizi katika bahari kuu miongoni mwa mashetani maasi.

38 Na wengine katika hao mashetani wamefungwa wao kwa wao kwa minyororo, kuwazuia na wengine wenasifanye ufasadi wao.

39. Hichi ndicho kipawa chetu. Basi toa au zuia, bila ya hisabu.³⁹
40. Na hakika yeye kwetu Sisi ana cheo cha kukaribishwa kwetu, na pahala pazuri pa kurejea.⁴⁰
41. Na mkumbuke mja wetu Ayubu alipo mwita Mola wake Mlezi akasema: Kwa hakika Shet'ani amenifikishia udhia na adhabu.⁴¹
42. (Akaambiwa:) Piga-piga ardhi kwa mguu wako! Basi haya maji baridi ya kuogea na ya kunywa.⁴²
43. Na tukampa ahali zake na wengine kama wao pamoja nao, kuwa ni rehema itokayo kwetu, na iwe kumbusho kwa watu wenye akili.⁴³
44. Na shika kicha cha vijiti tu mkononi mwako, kisha ndio upigie nacho, wala usivunje kiapo. Hakika tulimkuta mwenye subira, mbora wa waja, kwa hakika alikuwa mwingi wa kutubu.⁴⁴
45. Na wakumbuke waja wetu, Ibrahim na Is-haqa na Yaa'qubu walio kuwa na nguvu na busara.⁴⁵
46. Sisi tumewakhusisha wao kwa sifa ya ukumbusho wa Akhera.⁴⁶
47. Na hakika wao kwetu sisi ni wateuliwa walio bora.⁴⁷
48. Na mkumbuke Ismail na Alyasaa na Dhulkifli, na wote hao ni katika walio bora.⁴⁸
49. Huu ni ukumbusho. Na hakika wachamngu wana marudio mazuri.⁴⁹
50. Bustani za milele zitazo funguliwa milango yao kwa ajili yao.⁵⁰
51. Humo wataegemea matakia, wawe wanaagiza humo matunda mengi na vinywaji.⁵¹

39 Na akamfunulia kwa wahyi : Haya tuliyo kuneemesha kwayo ni kipawa kilicho toka kwetu. Yaani ni Sisi tulio kupa. Basi mpe umtakaye, na mnyime umtakaye. Hapana hisabu juu yako kwa kutoa au kunyima.

40 Hakika Suleiman kwetu Sisi ana ukaribisho mkubwa, na marejeo mazuri.

41 Ewe Muhammad! Mkumbuke mja wetu Ayubu alipo mwomba Mola wake Mlezi kwa kusema: Hakika Shetani amenipatisha taabu na machungu.

42 Tukamuitikia na tukamwambia: Ipige ardhi kwa mguu wako, yatatimbuka maji baridi, utakoga na utakunywa hayo, na kwa hivyo yatakuondokea machofu na adhabu.

43 Tukamkusanyia watu wake walio kuwa wametapanyika mbali naye siku zile za mateso yake. Na tukamzidishia wengine wama wale. Na tulifanya hayo kuwa ni rehema kutokana nasi, na ili yawe ni mawaidha kwa wenye akili, wapatte kujua kuwa matokeo ya subira ni faraji.

44 Ayubu alikuwa kaapa kuwa atampiga mmoja wapo katika ahali zake fimbo kadhaa wa kadhaa. Mwenyezi Mungu alimhalalishia aondoe kiapo chake kwa kuchukua kifungu cha fimbo idadi ile ile alio apia kuwa atampigia. Basi kwa kile kifungu cha fimbo ampige aliye apa kuwa atampiga, na hapo yamini yake itakuwa imetimia kwa uchache wa machungu. Mwenyezi Mungu ndiye aliye mneemesha kwa neema hizi, kwa sababu Mwenyezi Mungu alimwona kuwa ni mtu aliye vumilia masaibu yake. Kwa hivyo amestahiki sifa. Mbora wa kusifiwa kwa ibada ni yeye, kwa sababu yeye ni mwingi mno wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu katika kila jambo.

45 Na mkumbuke mja wetu Ibrahim, na Is-haqa, na Yaa'qubu, wenye nguvu katika Dini na dunia, na wenye busara ya mwangaza.

46 Hakika Sisi tumewakhusisha wao kwa sifa, nayo ni kuwa wanaikumbuka Nyumba ya Akhera, wao wanaikumbuka nao wanakumbukwa kwayo.

47 Na hakika wao kwetu Sisi ni wenye kukhitarwa walio bora.

48 Na mkumbuke Ismail, na Alyasaa, na Dhulkifli - na wote hao ni miongoni mwa walio bora.

49 Haya tuliyo kusimulia ni khabari za baadhi ya Mitume ili kukukumbusha wewe na kuwakumbusha watu wako. Na hakika wachamngu walio jikinga na kumuasi Mwenyezi Mungu Mtukufu watapata marejeo mazuri na natija njema.

50 Wameandaliwa bustani za milele zilizo funguliwa milango yao hapana wa kuwazuia wasiingie humo.

51 Watakuwa wamekaa humo wakiegemea juu ya makochi na vitanda kama wafanyavyo wenye taanusi,

52. Na pamoja nao wake zao wenye kutuliza macho, hirimu zao.⁵²
53. Haya ndiyo mliyo ahidiwa kwa Siku ya Hisabu.⁵³
54. Hakika hii ndiyo riziki yetu isiyo malizika.⁵⁴
55. Ndio hivi! Na hakika wenye kuasi bila ya shaka watapata marudio maovu kabisa.⁵⁵
56. Nayo ni Jahannamu! Wataingia humo. Nacho hicho ni kitanda kiovu mno cha kulalia.⁵⁶
57. Ndio hivi! Basi na wayaonje maji ya moto na ya usaha!⁵⁷
58. Na adhabu nyenginezo za namna hii.⁵⁸
59. Hili ndilo kundi litakalo ingia pamoja nanyi. Hapana makaribisho mema kwao. Hakika hao wanaingia Motoni.⁵⁹
60. Waseme: Lakini nyinyi! Hamna mapokezi mazuri! Nyinyi ndio mlio tusabibisha haya, napo ni pahala paovu kabisa!⁶⁰
61. Waseme: Mola wetu Mlezi! Aliye tusabibisha haya mzidishie adhabu mara mbili Motoni.⁶¹
62. Watasema: Tuna nini hata hatuwaoni wale watu ambao tukiwahisabu ndio katika waovu?⁶²
63. Tulikosea tulipo wafanyia maskhara, au macho yetu tu hayawaoni?⁶³
64. Hakika hayo bila ya shaka ndiyo makhasimiano ya watu wa Motoni.⁶⁴
65. Sema: Hakika mimi ni mwonyaji tu; na hapana mungu ila Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenda nguvu,⁶⁵
66. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na viliomo baina yake, Mwenye nguvu, Mwenye

wakistarehe kwa kutaka matunda ya kila namna na vinywaji.

52 Na huko Peponi watakuwa na wake ambao macho yao hayawatazami ila waume zao tu, hawawaangalii wengineo, nao ni wa miaka sawa na waume zao. Kwa hivyo wameelekeana kuwafikiana.

53 Raha hii ndiyo mliyo ahidiwa kuipata Siku ya Kiyama.

54 Hakika haya bila ya shaka ni tunayo yatoa Sisi, na wala hayana ukomo.

55 Neema hizi ni malipo ya wachamngu. Na hakika majabari wenye kuwaasi Manabii wao bila ya shaka watakuwa na marejeo na mwisho muovu.

56 . Na mwisho huo ni Jahannamu watakayo iingia, na moto wake uwatese. Na malalio maovu mno hayo!

57 Haya maji ya moto, mwisho wa umoto, na usaha wa watu wa Jahannamu wataamrisha wayaonje.

58 Na adhabu nyengine mfano wa hizi, za namna kwa namna zilizo changanyika.

59 Na majabari, wale marais wa washirikina, wataambiwa: Hawa chungu ya watu wanao ingia Motoni pamoja nanyi kwa kusukumana na kwa shida, ni wafwasi wenu. Wale marais watasema: Hawana mapokezi mema hao! Hakika hao wanaingia Motoni wapate kuteseka kwa mvukuto wake.

60 Na wafwasi hao watasema: Bali nyinyi ndio mnastahiki zaidi hayo maapizo mnayo tuapizia sisi, kwani nyinyi ndio mlio tuletea adhabu hii kwa vile mlivyo tudanganya na mkatuitia ukafirini, nasi tukakufuru kwa sababu yenu. Basi nyumba ovu kabisa ya kukaa ni Jahannamu!

61 Wafwasi watasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Aliye kuwa ni sababu ya adhabu hii, mzidishie adhabu mara mbili katika Moto.

62 Na watu wa Motoni watasema: Mbona hatuwaoni wale watu ambao tulikuwa duniani tukiwahisabu kuwa ndio katika waovu, na wa duni, wasio kuwa na jema lolote? Na watu hao ni wale mafakiri wa Kiislamu.

63 . Imekuwaje kuwa sisi tukiwakejeli na wala hawakuingia Motoni pamoja nasi? Au wamekwisha ingia na macho yetu yakazibwa tusiwaone tu?

64 Hakika hayo tuliyo yataja ya hadithi ya watu wa Motoni ni kweli ambayo haina budi kutokea, nayo ni ya kugombana kwa watu wa Motoni wao kwa wao.

65 Ewe Muhammad! Waambie washirikina: Hakika mimi ni mwenye kukuonyeni na adhabu ya Mwenyezi Mungu, na hapana wa kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu Mmoja ambaye hana mshirika wake, Mtenda nguvu, Mwenye kumshinda kila mwenye madaraka.

kusamehe.⁶⁶

67. Sema: Hii ni khabari kubwa kabisa.⁶⁷

68. Ambayo nyinyi mnaipuuza.⁶⁸

69. Sikuwa na ilimu ya mambo ya viumbe wakuu watukufu walipo kuwa wakishindana.⁶⁹

70. Haikufunuliwa kwangu isipo kuwa ya kwamba hakika mimi ni mwonyaji dhaahiri.⁷⁰

71. Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Hakika Mimi nitaumba mtu kutokana na udongo.⁷¹

72. Na nitakapo mkamilisha na kumpulizia roho inayo tokana nami, basi muangukieni kwa kumt'ii.⁷²

73. Basi Malaika wakat'ii wote pamoja.⁷³

74. Isipo kuwa Iblisi; alijivuna na akawa katika makafiri.⁷⁴

75. Mwenyezi Mungu akamwambia: Ewe Iblisi! Kipi kilicho kuzuia kumt'ii yule niliye muumba kwa mikono yangu? Je! Umejiona mkubwa, au umekuwa katika wakuu kweli?⁷⁵

76. Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, na yeye umemuumba kwa udongo.⁷⁶

77. Akasema: Basi toka humo, kwani hakika wewe umelaanika.⁷⁷

78. Na hakika laana yangu itakuwa juu yako mpaka Siku ya Malipo.⁷⁸

79. Akasema: Mola wangu Mlezi! Nipe muhula mpaka siku watayo fufuliwa viumbe.⁷⁹

80. Mwenyezi Mungu akasema: Basi umekwisha kuwa miongoni mwa walio pewa

66 Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na viliomo baina yao, Mwenye nguvu asiye shindika, Mwenye kusamehe, akazifuta dhambi za mwenye kumuamini.

67 Ewe Muhammad! Waambie: Haya ninayo kuambieni ni khabari kubwa, ambazo nyinyi mnazipuza. Msizikanye!

68 Tazama tanbihi ya 67.

69. Mimi sikuwa nikijua khabari za watukufu walio juu walipo kuwa wakizozana juu ya shauri ya Adam, kwa sababu mimi sikupitia njia za kupata ilimu zilizo zowewa na watu za kusoma vitabu au kupokea masomo kwa wataalamu. Njia yangu mimi ya kujua ni kwa kufunuliwa kwa Wahyi.

70 Na mimi sikufunuliwa kwa Wahyi ila kwamba hakika mimi ni Mtume wa kukufikishieni Ujumbe wa Mola wangu Mlezi kwa njia iliyo wazi kabisa.

71 Watajje pale alipo sema Mola wako Mlezi kuwaambia Malaika: Mimi nataka umbwa mtu, naye ni Adam a.s., kutokana na udongo.

72 Nikisha timiza kumuumba na nikampulizia siri ya uhai, nayo ni roho, muangukieni kwa kusujudi sijida ya kumtukua na kumuamkia.

73 Malaika wote wakafanya kama walivyo amrisha, wakamuangukia wakisujudi, isipo kuwa Iblisi. Yeye hakusujudi, na akajiona bora na akapanda kiburi, na akawa miongoni mwa makafiri.

74 Tazama tanbihi ya 73.

75 Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: Ewe Iblisi! Nini kilicho kuzuia kumsujudia niliye muumba Mimi mwenyewe bila ya kuingiliwa na yeyote kati yake! Umejiona mkubwa hali nawe si mkubwa, au hakika wewe nafsi yako ni katika walio shinda ukubwa?

76. Iblisi akasema: Mimi ni bora kuliko Adam; kwani Wewe umeniumba kwa moto, na yeye umemuumba kwa udongo. Basi vipi mimi nimsujudie yeye?

77 Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kumlipa Iblisi kwa kiburi chake cha kukataa amri ya Mola wake Mlezi, alimwambia: Basi toka kwenye kundi la watukufu walio juu, kwani wewe umekwisha fukuzwa kutokana na rehema yangu!

78 Na hakika wewe umetengwa mbali na kila kheri mpaka Siku ya Malipo. Hapo utalipwa kwa sababu ya kunikufuru Mimi na kunifanyia kiburi.

79 Iblisi akasema: Mola Mlezi! Nipe muhula, wala usinifishe mpaka Siku ya kufufuliwa viumbe

muhula,⁸⁰

81. Mpaka siku ya wakati maalumu.⁸¹

82. Akasema (Iblisi): Naapa kwa utukufu wako, bila ya shaka nitawapoteza wote,⁸²

83. Isipo kuwa wale waja wako miongoni mwao walio khitariwa.⁸³

84. Akasema: Haki! Na haki ninaisema.⁸⁴

85. Bila ya shaka nitaijaza Jahannamu kwa wewe na kwa hao wote wenye kukufuata miongoni mwao.⁸⁵

86. Sema (Ewe Mtume) : Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu.⁸⁶

87. Hayakuwa haya ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.⁸⁷

88. Na bila ya shaka mtajua khabari zake baada ya muda.⁸⁸

80 Akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Basi wewe utaakhirishwa, utapewa muhula, mpaka siku ya wakati tunao ujua Sisi, nao ni kumalizika dunia.

81 Tazama tanbihi ya 80.

82 Iblisi akasema: Basi naapa kwa Ukubwa wako na Utukufu wako, kwa yakini nitawapoteza watu wote, isipo kuwa waja wako ulio wateuwa kwa ajili ya kukut'ii Wewe. Hao sina madaraka nao.

83 Tazama tanbihi ya 82.

84 Akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Haki ndiyo yamini yangu na kiapo changu; na wala sisemi ila Haki. Bila ya shaka nitaijaza Jahannamu kwa jinsi yako ya kishetani na watakao kufuata katika vizazi vya Adam wote. Hapana khitalafu kwangu baina ya wafuasi na wanao fuatwa.

85 Tazama tanbihi ya 84.

86 Ewe Muhammad! Waambie umma wako: Mimi sikuombeni ujira kwa ajili ya haya niliyo amrisha nikufikishieni yaliyomo katika Qur'ani na Wahyi. Wala mimi si katika hao wanao jipamba na yasiyo kuwa yao, hata nijidai Unabii.

87 Haikuwa Qur'ani ila ni ukumbusho na mawaidha kwa walimwengu wote.

88 Na hapana shaka nyinyi, mnao ikadhibisha Qur'ani, mtakuja jua karibuni hivi ukweli uliomo ndani yake wa ahadi, na maonyo, na khabari za mambo yatakayo kuja, na Ishara za ulimwengu.

Sura 39 - Azzumar

Utangulizi

Sura hii ni ya Makka, yasemekana, isipo kuwa Aya 52, 53 na 54. Na Aya zake ni 75. Imefunguliwa Sura hii kwa kuisifu Qur'ani, kisha kwa kuwataka watu wamsafie ibada Mwenyezi Mungu peke yake, na inawarudi wale wanao sema kwamba Mwenyezi ana mwana. Kisha Aya zikaeleza uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kuumba mbingu na ardhi, na kumuumba mtu; na kwamba watu wakimkanya Yeye basi Yeye si mwenye kuwahitajia wao, na kwamba wakimshukuru, Yeye huwa radhi nao, na wala hawaridhii wakimkanusha. Na kadhaalika Sura hii imeeleza khulka ya binaadamu katika hali mbili, yaani anapo patwa na shida humwomba Mola wake na akarejea kwake, na akimneemsha mara husahau yale aliyo kuwa akiyaomba kabla yake.

Kisha Sura ikaunganisha makhusiano baina ya anaye tahadhari na Akhera na akataraji rehema ya Mola wake Mlezi, na wale wanao muasi; na malipo aliyo waandalia hawa na wale kwa Siku ya Kiyama. Kisha inawakumbusha neema za Mwenyezi Mungu kwa kuwateremshia maji, na kwamba Yeye huihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na huotesha mimea ambayo inapitia viwango mbali mbali. Na katika hayo yapo makumbusho kwa wenye akili.

Kisha Sura inarejea kusimulia khabari ya Qur'ani na athari zake kwa wanao mwegopa Mola wao Mlezi. Na kwamba Mwenyezi Mungu kawapigia mifano ndani yake ili wazingatie, hiyo ni Qur'ani isio na pogo ili wamchemungu. Kisha Sura ikalinganisha baina ya mja mshirikina na mja mwenye kumtakasisha Mwenyezi Mungu kwa ibada, na kuwa hakika hawa wawili hawawi sawa. Na kuwa hakika mauti ndio mwisho wa wote, na baadae mbele ya Mola wao Mlezi ndio watazozana.

Kisha Sura ikabainisha mwisho wa mwenye kumzulia uwongo Mwenyezi Mungu na akaikadhibisha kweli, na mwisho wa wasemao kauli ya kweli, wenye kusadiki waliyo teremshiwa. Na hakika hao washirikina ukiwauliza: Nani aliye umba mbingu na ardhi? Hapana shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Lakini nao juu ya hayo wanawaabudu wasio walinda na madhara pindi Mwenyezi Mungu akitaka kuwadhuru, wala hawaizuii rehema ya Mwenyezi Mungu pindi akiwataki rehema. Tena Sura hii inathibitisha kwamba Kitabu hichi kimeteremshwa kwa haki. Basi mwenye kuongoka ni kwa maslaha ya nafsi yake, na mwenye kupotea dhambi zake ni juu ya nafsi yake. Na hakika Mtume s.a.w. si mwakilishi juu yao.

Kisha Sura inarejea kuwakumbusha kufa na kufufuliwa, na kwamba wale miungu ya kishirikina (ya kipagani) walio wafuata badala ya Mwenyezi Mungu hawawafai kitu, hata kuwaombea. Kwani hakika uombezi wote uko kwa Mwenyezi Mungu.

Na yalipo kithiri maneno juu ya adhabu chungu walio andaliwa waasi na waharibifu - na labda haya ndiyo yaliyo zipelekea nyoyo zao kukata tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu - amewafungulia mlango wa kutumai rehema yake kwa kusema: "Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Msamehevu Mwenye kurehemu." Na akawataka warejee kwake kabla haijawajia adhabu kwa ghafla na wao hawatambui: "Na Siku ya Kiyama utawaona wale walio msingizia uwongo Mwenyezi Mungu nyuso zao zimesawijika. Je! Si katika Jahannamu

makaazi ya wale wanao takabari?” Na wenye kuchamngu halitawagusa oву, na wala hawatahuzunika. Na Sura ikakhitimisha kwa kusimulia khabari za Siku ya Mwisho, tangu mwanzo wake litapo pulizwa barugumu wakapigwa bumbuazi walioko mbinguni na kwenye ardhi isipo kuwa wale ambao Mwenyezi Mungu amewatakia. Mpaka pale kila mwenye haki akaitwaa haki yake. Tena wakasukumwa watu wa Motoni wende Motoni, na watu wa Peponi wakapelekwa huko. Nao hao waseme: Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliye timiza ahadi yake, na akawahukumia wote kwa haki, na ikasemwa: *Alhamdulillah Rabbi'la'alamiin*. Sifa njema zote ni za Mola Mlezi wa viumbe vyote

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Mteremsho wa Kitabu hiki umetokana na Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹
2. Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa Haki. Basi muabudu Mwenyezi Mungu ukimsafia Dini Yeye tu.²
3. Hakika Dini Safi ni ya Mwenyezi Mungu tu. Na wale wanao wafanya wenginewe kuwa ni walinzi wakisema: Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu - Hakika Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao katika wanayo khitalifiana. Hakika Mwenyezi Mungu hamwongoi aliye mwongo kafiri.³
4. Lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka kuwa na mwana, basi bila ya shaka angeli teua amtakaye katika alio waumba. *Subhanahu*, Ametakasika na hayo! Yeye ni Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenda atakalo.⁴
5. Ameumba mbingu na ardhi kwa Haki. Hufunika usiku juu ya mchana, na hufunika mchana juu ya usiku. Na amefanya jua na mwezi vitumike. Kila kimojapo kinakwenda kwa kipindi kilicho wekewa. Jueni mtanabahi! Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kusamehe!⁵

1 Qur'ani imeteremka kutokana na Mwenyezi Mungu, ambaye hana wa kumshinda kwa atakayo; Mwenye hikima katika vitendo vyake na utungaji wa sharia zake.

2 Hakika Sisi tumekuteremshia wewe, Muhammad, Qur'ani hii yenye kuamrisha Haki. Basi muabudu Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia ibada Yeye tu peke yake.

3 Jueni na mtambue kwamba Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye Dini isiyo kuwa na ila. Na washirikina walio wafanya wenginewe kuwa ni wasaidizi wa kuwanusuru, wanasema: Sisi hatuwaabudu hawa kwa kuwa ni waumbaji, bali tunawaabudu wapate kutukaribisha kwa Mwenyezi Mungu, kwa mkaribisho wa kutuomba sisi kwake Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu atahukumu baina ya hawa washirikina na Waumini wenye kumuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja katika yale wanayo khitalifiana katika matatizo ya shiriki na Tawhidi. Hakika Mwenyezi Mungu hamjaalii afikie Haki mtu ambaye mtindo wake ni uwongo na kukanya.

4 Lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka kuwa na mwana, kama wasemavyo Wakristo kwa Masihi, na washirikina kwa Malaika, basi angeli jichagulia amtakaye katika viumbe vyake, la sio kama mtakavyo nyinyi. Mwenyezi Mungu ametakasika na upungufu wa kuhitajia mwana. Yeye ni Mwenyezi Mungu asiye kuwa na mfano kama Yeye. Mtenda kama apendavyo, ukomo wa kutenda.

5 Ameumba mbingu na ardhi kwa kushikamana na Haki na kuwa sawa kwa kufuatana na sharia zilizo thibiti. Usiku unaufunika mchana, na mchana unaufunika usiku kwa mfululizo. Na amedhalilisha jua na mwezi kwa mujibu atakavyo na kwa mujibu wa maslaha ya waja wake. Kila kimojapo katika hivyo

6. Amekuumbeni kutokana na nafsi moja. Kisha akamfanya mwenziwe katika nafsi ile ile. Na akakuleteeni wanyama wa mifugo jozi nane. Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu, umbo baada ya umbo, katika viza vitatu. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Ufalme ni wake. Hapana mungu isipo kuwa Yeye. Basi nyinyi mnageuzwa wapi?⁶

7. Mkikufuru basi Mwenyezi Mungu si mwenye haja nanyi, lakini hafurahii kufuru kwa waja wake. Na mkishukuru Yeye hufurahika nanyi. Wala mbebaji habebi mzigo wa mwingine. Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu Mlezi. Hapo atakwambieni mliyo kuwa mkiyafanya. Hakika Yeye ni Mwenye kuyajua vyema yaliyomo vifuani.⁷

8. Na taabu inapo mfikia mtu humwomba Mola wake Mlezi naye ameelekea kwake. Kisha akimpa neema kutoka kwake, husahau yale aliyo kuwa akimwitia zamani, na akamfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze watu njia yake. Sema: Starehe na ukafiri wako kwa muda mchache. Kwani hakika wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.⁸

9. Je! Afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama akitahadhari na Akhera, na akitaraji rehema za Mola wake Mlezi...Sema: Ati watakuwa sawa wale wanao jua na wale wasio jua? Hakika wanao kumbuka ni watu wenye akili.⁹

10. Sema: Enyi waja wangu mlio amini! Mcheni Mola wenu Mlezi. Wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema. Na ardhi ya Mwenyezi Mungu ni kunjufu.

vinakwenda katika njia yake mpaka ufike wakati aliyo uwekea Yeye, nao ni Siku ya Kiyama. Jueni basi kuwa Yeye tu, si mwenginewe, ndiye Mwenye kushinda kila kitu. Basi hapana kitu chochote kilicho tokana na atakavyo Yeye, ambaye amefikilia ukomo wa kuwasamehe wenye kutenda madhambi katika waja wake. (*Tazama Maelezo 39:5*)

6 Enyi watu! Mwenyezi Mungu amekuumbeni kutokana na nafsi moja, naye ni Adam, baba wa watu wote. Na amemuumba kutokana na nafsi hiyo mkewe, Hawa. Na amekuteremshieni kwa ajili ya maslaha yenu namna nane za nyama hoa, wanyama wa mifugo, madume na majike. Nao ni ngamia, na ng'ombe, na kondoo, na mbuzi. Naye anakuumbeni matumboni mwa mama zenu kwa kukua na kugeuka geuka, katika viza vitatu, navyo ni kiza cha tumbo, na tumbo la uzazi, na zalio. Huyu aliye kuneemesheni kwa neema hizi ndiye Mwenyezi Mungu, Mlezi wenu, Mwenye kumiliki mambo yenu yote. Ni Yeye tu, si mwenginewe, ndiye Mwenye utawala wa pekee. Hapana wa kuabudiwa kwa Haki ila Yeye. Basi yawaje hata wanaacha kumuabudu Yeye wakenda kuwaabudu wenginewe? (*Tazama Maelezo 39:6*)

7 Enyi watu! Mkizikataa neema za Mwenyezi Mungu, basi Yeye hakika si mhitaji wa imani yenu na shukrani zenu. Lakini Yeye hapendi waja wake wakufuru, kwa sababu hayo yanawadhuru wenyewe. Na mkimshukuru kwa ajili ya neema zake, Yeye huwa radhi nanyi kwa shukra hiyo. Wala mtu mwenye madhambi hayabebi madhambi ya mwenginewe. Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu Mlezi, na hapo atakwambieni mliyo kuwa mkiyatenda duniani. Hakika Yeye anayajua mnayo yaficha katika nyoyo zenu ziliomo vifuani. (*Tazama Maelezo 39:7*)

8 Na mtu akifikiwa na shida yoyote katika shida za dunia humwomba Mola wake Mlezi, na hurejea kwake, baada ya kuwa akimpuza. Kisha Mola wake Mlezi akimpa neema kubwa husahau zile taabu alizo kuwa akimwomba Mola wake Mlezi amwondolee na amfarije kabla hajamneemsha kwa neema hizo. Na humfanyia Mwenyezi Mungu miungu washirika walio sawa na Yeye kwa kuwaabudu. Huyu mtu hufanya haya ili ajipoteze yeye na wenginewe waiache Njia ya Mwenyezi Mungu. Ewe Muhammad! Mwambie huyo mwenye sifa hizi kwa kumwonya: Starehe na huko kuzikanya kwako neema za Mwenyezi Mungu zililo juu yako kwa muda mchache. Kwani hakika wewe ni katika watu wa Motoni.

9 Je! Mwenye kumnyenyekea Mwenyezi Mungu nyakati za usiku anao upitisha na hali yeye yumo kusujudu na kusimama, akiiogopa Akhera, naye anataraji rehema ya Mola wake Mlezi, ni kama anaye mwomba Mola wake Mlezi wakati wa shida na akamsahau wakati wa neema? Ewe Muhammad! Waambie: Ati wanakuwa sawa wenye kujua haki za Mwenyezi Mungu wakamuabudu Yeye tu peke yake, na wale wasio jua wakapuza kuziangalia Ishara? Hakika wenye akili nzuri ndio wanao waidhika.

Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu.¹⁰

11. Sema: Hakika mimi nimeamrisha nimuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia Dini Yeye tu.¹¹

12. Na nimeamrisha niwe wa mwanzo wa Waislamu.¹²

13. Sema: Hakika mimi ninaogopa adhabu ya Siku Kubwa nikimuasi Mola wangu Mlezi.¹³

14. Sema: Mwenyezi Mungu tu namuabudu kwa kumsafishia Yeye tu Dini yangu.¹⁴

15. Basi nyinyi abuduni mpendacho badala yake Yeye. Sema: Hakika walio khasirika ni wale walio jikhasiri nafsi zao na ahali zao Siku ya Kiyama. Tambueni kuwa hiyo ndiyo khasara iliyo dhaahiri.¹⁵

16. Yatawekwa juu yao mat'abaka ya moto, na chini yao mat'abaka. Kwa hayo Mwenyezi Mungu anawakhofisha waja wake. Enyi waja wangu! Nicheni Mimi!¹⁶

17. Na wale wanao jiepisha na ibada potovu, na wakarejea kwa Mwenyezi Mungu, watapata bishara njema. Basi wabashirie waja wangu.¹⁷

18. Ambao husikiliza maneno, wakafuata lilio bora yao. Hao ndio alio waongoa Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye akili.¹⁸

19. Je! Yule mwenye kustahiki hukumu ya adhabu, je, wewe unaweza kumwokoza aliyomo katika Moto?¹⁹

20. Lakini walio mcha Mola wao Mlezi watapata ghorofa zilizo jengwa juu ya ghorofa; chini yake hupita mito. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji

10 Ewe Nabii! Sema kwa kufikisha Ujumbe unao toka kwa Mola wako Mlezi: Enyi waja wangu mlio niamini! Jikingeni na ghadhabu za Mola wenu Mlezi. Mwenye kutenda mema atalipwa mema, duniani kwa kusaidiwa, na Akhera kwa Pepo. Wala msikae katika unyonge, kwani ardhi ya Mwenyezi Mungu ina wasaa. Na subirini kwa kufarikiana na nchi zenu na wapenzi wenu. Kwani hakika Mwenyezi Mungu huwalipa wenye kusubiri ujira wao mara zisio ingia katika hisabu za wanao hisabu.

11 Sema: Mimi nimeamrisha nimuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumsafia ibada yangu isiwe na shirki ndani yake wala riya ya kujionyesha kwa watu.

12 Na nimeamrisha amri iliyo tokana naye Mtukufu, amri ya nguvu, ya kwamba niwe wa mwanzo wa kufuata amri zake.

13 Sema: Mimi naogopa adhabu ya Siku Kubwa yenye vitisho ikiwa nitamuasi Mola wangu Mlezi.

14 Ewe Muhammad! Waambie: Ninamuabudu Mwenyezi Mungu peke yake, na ibada yangu haina shirki wala riya. Na nyinyi ikiwa mnajua Njia yangu nanyi hamnit'ii, basi abuduni mpendacho badala yake Yeye. Waambie: Hakika wenye kupata khasara ni wale walio jitupa kwa upotovu wao wenyewe, na wakawatupa ahali zao kwa kuwapoteza wao Siku ya Kiyama. Ama hakika kupotoka huko ndio khasara iliyo timia na iliyo dhaahiri.

15 Tazama tanbihi ya 14.

16 Hawa walio khasirika watakuwa na mat'abaka ya Moto yalio rindikwa juu yao, na chini yao hali kadhaalika. Kwa namna ya adhabu hiyo ndio Mwenyezi Mungu anawahadharisha waja wake. Enyi waja wangu! Basi yaogopeni mateso yangu.

17 Na wale wanao jitenga na masanamu na mashet'ani wasiyakurubie, na wakarejea kwa Mwenyezi Mungu katika mambo yao yote, wanayo bishara tukufu katika mwahala mote. Basi Ewe Muhammad! Wape bishara nzuri waja wangu wanao sikiliza kauli na wakaifuata iliyo bora na yenye kuwaongoa kwendea katika Haki. Hao tu, si wenginewe, ndio Mwenyezi Mungu atao wafikisha kwenye Uwongofu. Na hao tu, si wenginewe, ndio wenye akili zilizo nawirika.

18 Tazama tanbihi ya 17.

19 Je! Unaweza kuniingilia katika Ufalme wangu? Iliyo kwisha pita juu yake hukumu ya kumuadhibu, je, wewe unaweza kuizua? Unayo nguvu hiyo wewe? Je! Unaweza kuwaokoa na Moto baada ya kwisha wathibitikia?

ahadi yake.²⁰

21. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mbinguni. Kisha akayapitisha kwenye chemchem katika ardhi, kisha kwa maji hayo akatoa mimea yenye rangi mbali mbali? Kisha hunyauka ukaiona imekuwa kimanjano, na kisha huifanya mapepe. Bila ya shaka katika hayo upo ukumbusho kwa wenye akili.²¹

22. Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisio mkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri.²²

23. Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa; husisimua kwacho ngozi za wenye kumkhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Huo ndio uwongofu wa Mwenyezi Mungu, na kwa huo humwongoa amtakaye. Na ambaye ameachwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hapana wa kumwongoa.²³

24. Je! Atakaye kuwa anapambana kwa uso wake na adhabu mbaya kabisa Siku ya Kiyama (ni sawa na watenda wema?) Na wataambiwa wenye kudhulumu: Onjeni hayo mliyo kuwa mkiyachuma!²⁴

25. Walio kuwa kabla yao walikadhibisha , na ikawajia adhabu kutoka pahala wasipo patambua.²⁵

26. Basi Mwenyezi Mungu akawaonjesha hizaya katika uhai wa duniani. Na bila ya shaka adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi; laiti wangeli jua!²⁶

27. Na bila ya shaka tumewapigia watu mifano ya kila namna katika hii Qur'ani ili

20 Lakini wenye kumkhofu Mola wao Mlezi watapata vyeo vya juu Peponi na majumba yake ya fakhari, yenye kupitiwa chini yake na mito. Hiyo ni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu haendi kinyume na ahadi yake.

21 Ewe usemezwaye! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mbinguni, akayapitisha kwenye mito na chemchem za katika ardhi, kisha kwa maji hayo akaotesha mimea ya namna mbali mbali. Kisha baada ya kustawi kwake hiyo mimea, ikayabisika ukaiona imekuwa rangi ya manjano baada ya kustawi kwake. Kisha akaifanya imevurugika na kukatika vipande vipande. Hakika kutoka kwenye hali moja na kuingia hali nyengine ni mazingatio kwa wenye akili zilizo nawirika. (*Tazama Maelezo 39:21*)

22 Kwani watu wote ni sawa? Mwenye kufunguliwa kifua chake na Mwenyezi Mungu kwa Uislamu kwa kupokea mafunzo yake, na akawa na utambuzi unao tokana na Mola wake Mlezi, huyo basi ni kama yule anaye kataa kuangalia Ishara zake? Basi hao ambao nyoyo zao zimekuwa ngumu hata hawamkumbuki Mwenyezi Mungu watapata adhabu kali! Hao wenye nyoyo ngumu wameitupa Haki iliyo wazi.

23 Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa, nayo ni Kitabu ambacho zimeshabihiana maana zake na matamko yake kwa kufikilia ukomo wa kuwashinda watu kuleta mfano wake, na hukumu zake. Mawaidha na hukumu zinakaririwa, kama kunavyo kaririwa kusomwa kwake. Kinapo somwa Kitabu hicho na kikasikiwa maonyo yake, ngozi za wenye kumkhofu Mola wao Mlezi hukunjika, na kisha hulainika ngozi zao na nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hicho Kitabu kilicho kusanya sifa hizi ni Nuru ya Mwenyezi Mungu ambayo kwayo humwongoa amtakaye, ikamwezesha kufikilia kumuamini Yeye. Na anaye achwa na Mwenyezi Mungu apotee kwa kumjua kuwa tangu hapo ataiacha Haki, basi hapati mwongozi wa kumwokoa na upotofu wake.

24 Kwani watu wote ni sawa? Mwenye kuikinga adhabu oву, kali, kwa uso wake Siku ya Kiyama baada ya kuwa mikono yake imetiwa pingu, ni kama anaye kuja kwa amani Siku ya Kiyama? Na wenye kudhulumu wataambiwa: Onjeni laana ya vitendo vyenu!

25 Walikanusha walio kuja kabla ya washirikina hawa, ikawajia adhabu kutoka upande wasio utaraji.

26 Mwenyezi Mungu akawaonjesha unyonge katika maisha ya duniani. Ninaapa: Hakika adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi kuliko ya duniani, lau kwamba walikuwa ni watu wa kujua na kuangalia!

wapate kukumbuka.²⁷

28. Qur'ani ya Kiarabu isiyo na upogo, ili wamche Mungu.²⁸

29. Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mtu mwenye mabwana washirika wanagombana, na wa mtu mwengine aliye khusika na bwana mmoja tu. Je! Wako sawa katika hali zao? *Alhamdulillah*, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu! Lakini wengi wao hawajui.²⁹

30. Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa.³⁰

31. Kisha bila ya shaka mtagombana Siku ya Kiyama mbele ya Mola wenu Mlezi.³¹

32. BASI NI NANI dhaalimu mkubwa kuliko yule aliye msingizia uwongo Mwenyezi Mungu na kuikanusha kweli imfikiapo? Je! Siyo katika Jahannamu makaazi ya hao makafiri?³²

33. Na aliye ileta Kweli na akaithibitisha - hao ndio wachamngu.³³

34. Watapata watakacho taka kwa Mola wao Mlezi. Hayo ndiyo malipo ya watendao mema.³⁴

35. Ili Mwenyezi Mungu awafutie ukomo wa uovu walio ufanya na awalipe ujira wao kwa mujibu wa ukomo wa wema walio kuwa wakiutenda.³⁵

36. Je! Mwenyezi Mungu si wa kumtoshela mja wake? Na ati wanakutishia kwa hao wenginewe wasio kuwa Yeye! Na aliye hukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumwongoa.³⁶

37. Na ambaye Mwenyezi Mungu anamwongoa hana wa kumpotoa. Je! Mwenyezi Mungu si Mwenye nguvu anaye weza kulipiza?³⁷

27 Na bila ya shaka tulikwisha wabainishia watu katika hii Qur'ani kwa kila mfano wa kuwakumbusha Haki, kwa kutaraji kuwa watakumbuka na watawaidhika.

28 Tumeiteremsha Qur'ani ya Kiarabu kwa ulimi wao, haina upungufu, kwa kutaraji kuwa watamcha na watamwogopa Mola wao Mlezi.

29 Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mshirikina kama mtumwa aliye milikiwa na watu kadhaa wenye kushirikiana, na wenye kumgombania. Na mfano wa mwenye kuamini Mwenyezi Mungu Mmoja kama mtu ambaye amemilikiwa na mtu mmoja tu. Je hao wanakuwa sawa? *Alhamdulillah* kwa kusimama hoja mbele ya watu. Lakini watu wengi hawajui Haki.

30 Hakika wewe, Muhammad, na wao wote mtakufa. Kisha baada ya kufa kwenu mtafululiwa mbele ya Mwenyezi Mungu mkishitakiana nyinyi kwa nyinyi.

31 Tazama tanbihi ya 30.

32 Basi hapana aliye dhaalimu mkubwa zaidi kuliko yule anaye msingizia Mwenyezi Mungu lisio kuwa lake, na akaikanusha Haki bila ya kufikiri wala kuzingatia pale inapo mjia kwa ndimi za Mitume. Kwani katika Jahannamu sio makaazi ya makafiri walio ghurika hata wakamfanyia jeuri Mwenyezi Mungu?

33 Na wale walio ileta Haki na wakaisadiki ilipo wajia, hao ndio wachamngu kweli, wala si wengineo.

34 Wachamngu hao watapata kutoka kwa Mola wao Mlezi kila wakipendacho. Fadhila hiyo ni malipo ya kila mwenye kufanya vizuri katika itikadi yake na vitendo vyake.

35 Mwenyezi Mungu amewakirimu wachamngu kwa alivyo wakirimu, ili awafutie vile vitendo vyao viovu kabisa, na awalipe ujira wao kwa bora ya vitendo vyao walivyo vitenda duniani.

36 Mwenyezi Mungu, peke yake, ni Mwenye kuwatosheleza waja wake kwa kila lilio wakhusu. Na ati hao makafiri wa Kikureshi wanakutisha, ewe Muhammad, kwa miungu yao wanayo iomba badala ya Mwenyezi Mungu. Na hayo ni katika upotovu wao. Na mwenye kupotozwa na Mwenyezi Mungu, kwa kumjua kuwa huyo amekhiari upotovu kuliko uwongofu, basi hatakuwa na mwongozi wa kumwongoza.

37 Na mwenye kuongozwa na Mwenyezi Mungu kuendea Haki, na akamwezesha kuifikia, kwa kujua kwake kuwa huyo amekhiari uwongofu kuliko upotovu, basi hatokuwapo wa kumpotoa akaiacha Njia ya Uwongofu. Kwani Mwenyezi Mungu si ndio Yeye ambaye hashindiki kwa kila upande, ambaye ni Mwenye kulipiza kwa ukali? Na kwa hivyo huwalinda vipenzi vyake na maadui wake?

38. Na ukiwauliza: Ni nani aliye ziumba mbingu na ardhi. Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Sema: Je! Mnawaonaje wale mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa Mwenyezi Mungu akitaka kunidhuru, wao wanaweza kuniondolea dhara yake? Au akitaka kunirehemu, je, wao wanaweza kuzuia rehema yake? Sema: Mwenyezi Mungu ananitosheleza. Kwake Yeye wategemee wanao tegemea.³⁸

39. Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni mwezavyo, mimi pia nafanya. Basi mtakuja ona³⁹

40. Ni nani itakaye mfikia adhabu ya kumhizi, na itakaye mshukia adhabu ya daima.⁴⁰

41. Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu kwa ajili ya watu wote kwa Haki. Basi mwenye kuongoka ni kwa nafsi yake, na mwenye kupotoka bila ya shaka amepotoka kwa khasara yake. Na wewe si mlinzi juu yao.⁴¹

42. Mwenyezi Mungu huzipokea roho zinapo kufa. Na zile zisio kufa wakati wa kulala kwake, huzishika zilizo hukumiwa kufa, na huzirudisha nyengine mpaka ufike wakati uliowekwa. Hakika katika hayo bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri.⁴²

43. Au ndio wanachukua waombezi badala ya Mwenyezi Mungu? Sema: Ingawa hawana mamlaka juu ya kitu chochote, wala hawatambui lolote?⁴³

44. Sema: Uombezi wote uko kwa Mwenyezi Mungu. Ni wake Yeye tu ufalme wa mbingu na ardhi. Kisha mtarejeshwa kwake.⁴⁴

45. Na anapo tajwa Mwenyezi Mungu peke yake nyoyo za wasio iamini Akhera huchafuka. Na wanapo tajwa wenginewe asiye kuwa Yeye basi wao hufurahi.⁴⁵

46. Sema: Ewe Mwenyezi Mungu! Muumba mbingu na ardhi! Mjuzi wa yasiyo onekana na yanayo onekana! Wewe utahukumu baina ya waja wako katika waliyo

38 Na ninaapa, lau ungesi wauliza, wewe Muhammad, hawa washirikina: Nani aliye ziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka wangu sema: Mwenyezi Mungu ndiye aliye ziumba. Ewe Muhammad, waambie: Mmazingatia mkawaona hao miungu mnao washirikisha na Mwenyezi Mungu, wanaweza kuniondolea madhara ikiwa Mwenyezi Mungu anataka kunidhuru? Au wanaweza kunizuilia rehema yake akitaka inifikie? Ewe Muhammad! Waambie: Anaye nitosheleza kwa kila kitu ni Yeyey peke yake, si mwenginewe, ndiye Yeye wanaye mtegemea wote wanao tegemea na kumwachilia kila kitu.

39 Waambie, kwa kuwapa ahadi: Enyi watu! Ishikilieni hiyo hiyo njia yenu ya ukafiri na kukadhibisha, na mimi hakika ninashikilia aliyo niamrisha Mola wangu Mlezi. Mtakuja ona nani katika sisi atakaye fikiwa na adhabu ya kumdhaliisha, na atakaye teremkiwa na adhabu ya daima isiyo mwondokea?

40 Tazama tanbihi ya 39.

41 Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekuteremshia Qur'ani Tukufu hii kwa watu wote, nayo imekusanya Haki iliyo thibiti. Basi mwenye kuongoka kwa sababu yake basi manufaa hayo ni kwa nafsi yake, na mwenye kuipotea njia yake basi balaa ya upotofu wake itamrejea mwenyewe. Wala wewe, Muhammad, si mwenye kuwakilishwa uwongofu wao. Jukumu lako ni kufikisha ujumbe, nao umeufikisha.

42 Mwenyezi Mungu huzitakabadhi roho zinapo kufa. Na huzipokea roho zisio kufa zinapo lala. Basi huzizuia zilizo kwisha hukumiwa kufa, zisirudi kwenye miili yao, na huzirudisha nyenginezo ambazo hazijafikilia bado ajali yao, wakati wa kuamka, mpaka itakapo fika ajali yao ilio wekewa. Hakika katika hayo bila ya shaka zipo Ishara wazi kwa watu wanao zingatia.

43 Bali washirikina wakawafanya wengineo badala ya Mwenyezi Mungu kuwa ni waombezi wao wa kuwakurubisha kwake. Waambie, ewe Muhammad: Mnafanya haya ijapo kuwa hawa mnao wafanya "waombezi" hawanacho wanacho kimiliki, wala hawana wanacho kifahamu?

44 Ewe Muhammad! Waambie: Uombezi wote uko kwa Mwenyezi Mungu peke yake! Hapana anaye upata ila aridhie Yeye. Ufalme wa mbingu na ardhi ni wake Yeye tu. Na kisha mtarejeshwa kwake, akuhisabieni vitendo vyenu.

45 Na pindi akitajwa Mwenyezi Mungu peke yake, bila ya kutajwa miungu yao, nyoyo za wasio yaamini maisha ya Akhera hukunjana na kukasirika. Na wakitajwa miungu yao wanayo iabudu badala ya Mwenyezi Mungu wao huwa wepesi kufurahi na kustarehe.

kuwa wakikhitalifiana.⁴⁶

47. Na lau kuwa walio dhulumu wangeli kuwa na vyote viliomo duniani na pamoja navyo vingine kama hivyo, bila ya shaka wangeli vitoa kujikomboa katika adhabu mbaya hiyo Siku ya Kiyama. Na yatawadhihirikia kwa Mwenyezi Mungu wasiyo kuwa wakiyatarajia.⁴⁷

48. Na utawadhihirikia ubaya wa waliyo yachuma, yatawazunguka waliyo kuwa wakiyafanyia mzaha.⁴⁸

49. Na dhara inapo mgusa mtu hutuomba. Kisha tunapo mpa neema zitokazo kwetu, husema: Nimepewa haya kwa sababu ya ilimu yangu. Sio! Huo ni mtihani! Lakini wengi wao hawajui!⁴⁹

50. Waliyasema haya waliyo kuwa kabla yao, lakini hayakuwafaa waliyo kuwa wakiyachuma.⁵⁰

51. Basi ukawasibu uovu wa waliyo yachuma. Na wale walio dhulumu miongoni mwa hawa utawasibu uovu wa waliyo yachuma vile vile. Nao si wenye kushinda.⁵¹

52. Kwani wao hawajui kwamba Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye na akamkadiria? Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao amini.⁵²

53. Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁵³

54. Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na silimuni kwake, kabla ya kukujieni adhabu. Kisha hapo hamtanusuriwa.⁵⁴

46 Ewe Muhammad! Sema, nawe umemwelekea Mola wako: Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe Muumba mbingu na ardhi bila ya mithali! Ewe Mjuzi wa siri na dhaahiri! Wewe peke yako, ndiye wa kuhukumu baina ya waja wako katika hayo wanayo khitalifiana katika mambo ya dunia na Akhera. Basi hukumu baina yangu na hawa washirikina.

47 Na lau kuwa hao walio jidhulumu nafsi zao kwa ushirikina wanamiliki vyote viliomo duniani na mara mbili kama hivyo, bila ya shaka wangeli vitoa kuwa ni fidia ya kujigombolea nafsi zao na adhabu waliyo andaliwa Siku ya Kiyama. Nao watakuja iona adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu ambayo haikupata kuwapitikia katika mawazo yao.

48 Na katika Siku hii ya leo utawadhihirikia uovu wa vitendo vyao, na itawazunguka adhabu ya yale waliyo kuwa wakiyafanyia maskaara duniani.

49 Na mtu yakimpata madhara hutuomba kwa unyenyekevu; kisha tukimpa neema kwa kumfadhili, mtu huyo huyo husema: Sikupewa neema hizi mimi ila kwa ujuzi wangu nilio nao wa kujua kuchuma. Naye mtu huyu kasahau kuwa mambo si hivyo kama asemavyo, bali neema hizo alizo mneemesha Mwenyezi Mungu ni kama majaribio tu, ni mtihani, ili amdhihirishe nani mwenye kut'ii na nani mwenye kua'si. Lakini wengi wa watu hawatambui kama hayo ni majaribio na fitna.

50 Maneno kama haya waliyasema walio kuwa kabla ya washirikina hawa, na hayakuwalinda na adhabu hayo mali na starehe waliyo yachuma.

51 Yakawasibu makafiri walio tangulia malipo ya madhambi ya vitendo vyao, na madhaalimu miongoni mwa hawa wanao semezwa hivi sasa yatawapata vile vile malipo ya madhambi ya vitendo vyao. Wala hawa hawataiepuka adhabu.

52 Je! Hawa wanasema wayasemayo, wala hawajui kwamba Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye katika waja wake, na humpa kwa kadiri atakacho kwa mujibu wa hikima yake? Hakika katika haya bila ya shaka ni mazingatio kwa watu wanao amini.

53 Ewe Muhammad! Sema kwa kufikisha kutokana na Mola wako Mlezi: Enyi waja wangu walio jizidishia juu ya nafsi zao maasi, msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huyafuta madhambi yote. Hakika Yeye, peke yake, ndiye Mkuu katika kusamehe kwake na kurehemu kwake.

54 Enyi mlio jidhulumu nafsi zenu, rejeeni kwa Mwenye kuyamiliki mambo yenu yote, na Mlezi wenu.

55. Na fuateni yaliyo bora kabisa katika yale yaliyo teremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi, kabla haijakujieni adhabu kwa ghafla, na hali hamtambui.⁵⁵
56. Isije ikasema nafsi: Ee majuto yangu kwa yale niliyo poteza upande wa Mwenyezi Mungu, na hakika nilikuwa miongoni mwa wanao fanya maskhara!⁵⁶
57. Au ikasema: Ingeli kuwa Mwenyezi Mungu ameniongoa, bila ya shaka ningeli kuwa miongoni mwa wenye kumchamngu.⁵⁷
58. Au ikasema inapo ona adhabu: Lau kuwa ningeli pata fursa nyengine, ningeli kuwa miongoni mwa wafanya mema.⁵⁸
59. Wapi! Bila ya shaka zilikuja Ishara zangu, nawe ukazikadhibisha, na ukajivuna, na ukawa miongoni mwa makafiri!⁵⁹
60. Na Siku ya Kiyama utawaona walio msingizia uwongo Mwenyezi Mungu nyuso zao zimesawijika. Je! Si katika Jahannamu makaazi ya wanao takabari?⁶⁰
61. Na Mwenyezi Mungu atawaokoa wenye kujikinga kwa ajili ya kufuzu kwao. Hapana uovu utao wagusa, wala hawatahuzunika.⁶¹
62. Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu, na Yeye ndiye Mlinzi juu ya kila kitu.⁶²
63. Yeye anazo funguo za mbingu na ardhi. Na wale walio zikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, hao ndio wenye kukhasiri.⁶³
64. Sema: Je! Mnaniamrisha nimuabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, enyi majaahili?⁶⁴

Na mfuateni Yeye kabla haijakujieni adhabu, tena hapo hapatakuwepo wa kukunusuruni na Mwenyezi Mungu na kukulindeni na adhabu yake.

55 Na fuateni yaliyo bora kabisa katika mliyo teremshiwa kutokana na Mola wenu Mlezi, nayo ni Qur'ani Tukufu, kabla ya kukujiieni adhabu kwa ghafla, na bila ya kujitayarisha, na hali nyinyi hamjui kuja kwake.

56 Rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na Msilimu kwake, na mfuate mafunzo yake, ili nafsi yenye dhambi isisema itapo iona adhabu: Ee msiba wangu kwa niliyo yawacha upande wa Mwenyezi Mungu na katika haki zake, na kwamba mimi nilikuwa duniani miongoni mwa walio kuwa wakiifanyia maskhara Dini yake.

57 Au iseme ile nafsi yenye dhambi, kutafuta udhuru: Lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli niwezesha kufuata uwongofu bila ya shaka ningeli kuwa duniani katika wale walio jilinda na adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa Imani na vitendo vyema

58 Au iseme nafsi ile yenye dhambi itapo ona adhabu: Laiti ningeli rejeshwa duniani, nikawa katika wanao tengeneza imani yao na vitendo vyao!

59 Utayapata wapi, ewe mwenye majuto! Mafunzo yangu yalikuja katika ndimi za Mitume, nawe ukayakanusha, na ukajiona bora, ukakataa kuyafuata, na ukawa katika dunia yako miongoni mwa wenye kushikilia ukafiri.

60 Na Siku ya Kiyama utawaona walio mzulia uwongo Mwenyezi Mungu, wakamkhusisha yasiyo kuwa yake, nyuso zao zimesawijika kwa huzuni na majonzi. Hakika Jahannamu ndio makaazi ya wenye kiburi wakaikataa Haki.

61 Na Mwenyezi Mungu atawaokoa alio wajaalia ulinzi isiwapate adhabu ya Mwenyezi Mungu, kwa vile alivyo kwisha wajua kuwa wamefuzu, kwa walivyo ukhari uwongofu kuliko upotofu. Na siku hii basi uovu hautawagusa, wala hawatahuzunika kwa kuzikosa neema walizo kuwa wakizitaraji.

62 Mwenyezi Mungu Muumba kila kitu - naye peke yake - ndiye Mlinzi wa kila kitu. Anaendesha mambo yake kwa mujibu wa hikima yake.

63 Maendesho ya mambo ya katika mbingu na ardhi yako kwa Mwenyezi Mungu. Hayaendeshi hayo isipo kuwa Yeye. Na makafiri kwa hoja za Mwenyezi Mungu na ushahidi wake ndio wao, peke yao, ndio wenye kukhasiri, mwisho wa kukhasiri! (*Tazama Maelezo 39:63*)

64 Ewe Muhammad! Sema: Je! Baada ya kuweka wazi Ishara zote kuwepo Mwenyezi Mungu Mmoja wa kuabudiwa, mnaniamrisha nimuabudu mwengine, enyi wajinga, majaahili?

65. Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa walio kuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu a'mali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri.⁶⁵

66. Bali muabudu Mwenyezi Mungu tu, na uwe miongoni mwa wenye kushukuru.⁶⁶

67. Na wala hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama anavyo stahiki kadiri yake. Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa mkononi mwake, na mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kuume. *Subhanahu wa Taa'la* Ametakasika na Ametukuka na hayo wanayo mshirikisha nayo.⁶⁷

68. Na litapulizwa barugumu, wazimie waliomo mbinguni na waliomo katika ardhi, isipo kuwa aliye mtaka Mwenyezi Mungu. Kisha litapulizwa mara nyengine. Hapo watainuka wawe wanangojea.⁶⁸

69. Na ardhi itang'ara kwa Nuru ya Mola wake Mlezi, na Kitabu kitawekwa, na wataletwa Manabii na mashahidi, na patahukumiwa baina yao kwa haki, wala hawatadhulumiwa.⁶⁹

70. Na kila nafsi italipwa kwa yale iliyo yafanya, na Yeye anayajua sana wanayo yatenda.⁷⁰

71. Na walio kufuru wataongozwa kuendea Jahannamu kwa makundi. Mpaka watakapo ifikia itafunguliwa milango yake, na walinzi wake watawaambia: Kwani hawakukujilieni Mitume miongoni mwenu wakikusomeeni Aya za Mola wenu Mlezi na kukuonyeni mkutano wa siku yenu hii? Watasema: Kwani! Lakini limekwisha thibiti neno la adhabu juu ya makafiri.⁷¹

72. Itasemwa: Ingieni milango ya Jahannamu mdumu humo. Basi nayo ni ubaya ulioje wa makaazi ya wanao takabari!⁷²

65 Na ninaapa: Bila ya shaka, umepewa Wahyi, wewe, Muhammad na Mitume walio kuwa kabla yako, kwamba bila ya shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote kile basi hapana shaka Mwenyezi Mungu atazibat' ilisha a'mali zako, na utakuwa katika watu walio khasirika ukomo wa kukhasiri.

66 Ewe Mtume! Usiwakubalie kwa hayo wanayo kutaka, bali muabudu Mwenyezi Mungu peke yake, na uwe katika wanao mshukuru Yeye kwa neema zake.

67 Washirikina hawakumtukuza Mwenyezi Mungu kama anavyo stahiki utukufu wake, wala hawakumjua kama anavyo stahiki kujuulikana, kwa kuwa wamemshirikisha pamoja naye wengine, na wakamtaka Mtume naye aingie katika ushirikina, na hali ardhi yote ni milki yake Siku ya Kiyama, na mbingu zitakuwa zimekunjwa, kama zinavyo kunjwa nguo, katika mkono wake wa kulia. Mwenyezi Mungu ametakasika na kila upungufu, na ametukuka vikubwa mno na vyote hivyo wanavyo mshirikisha naye.

68 Na litapulizwa barugumu kwa yakini, na watakufa walioko mbinguni na katika ardhi ila anaye mtaka Mwenyezi Mungu kumuakhirisha mpaka wakati mwengine. Kisha litapulizwa mara nyengine, na hapo wote watainuka kutoka makaburini mwao, walingojea watafanywa nini? (*Tazama Maelezo 39:68*)

69 Na ardhi itang'ara siku hiyo kwa nuru ya Muumba wake na Mmiliki wake. Na kitatayarishwa Kitabu kilicho sajiliwa ndani yake vitendo vyao, na watahudhurishwa Manabii na mashahidi wapate kuwashuhudia viumbe vyote, na wapambanuliwe baina ya viumbe kwa uadilifu, na wala hawatadhulumiwa kwa kupunguziwa thawabu wala kuzidishiwa adhabu.

70 Na kila nafsi itapewa malipo ya a'mali yake, na Mwenyezi Mungu ni mbora wa kujua vitendo vyao.

71 Na makafiri watahimizwa kwenda kwa nguvu kuendea Jahannamu kwa makundi makundi. Na hata watapo fika milango yake itafunguliwa, na walinzi wake watawaambia kwa kuwakebehi: Kwani hawakuja kwenu Wajumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu wa jinsi yenu, wakikusomeeni Aya za Mola wenu Mlezi, na wakakuhadharisheni na mkutano wenu huu? Makafiri watasema kwa kukiri: Kwani! Walitujia Mitume. Lakini neno la adhabu limekwisha wajibikia juu ya makafiri, kwa kuwa wao wamekhiari ukafiri kuliko Imani.

72 Wataambiwa: Iingieni milango ya Jahannamu mliyo jaaliwa mkae humo milele. Jahannamu ni pahala paovu mno pa kukaa wenye kutakabari na wakakataa kuikubali Haki.

73. Na walio mcha Mola wao Mlezi wataongozwa kuendea Peponi kwa makundi, mpaka watakapo fikilia, nayo milango yake imekwisha funguliwa. Walinzi wake watawaambia: *Salaam Alaikum*, Amani iwe juu yenu! Mmet'ahirika. Basi ingieni humu mkae milele.⁷³

74. Nao watasema: *Alhamdulillah*, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliye tutimizia ahadi yake, na akaturithisha ardhi, tunakaa katika Bustani popote tupendapo. Basi ni malipo mazuri yaliyoje ya watendao!⁷⁴

75. Na utawaona Malaika wakizunguka pembeni mwa Kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu, wakimtakasa na kumsifu Mola wao Mlezi. Na patahukumiwa baina yao kwa haki na patasemwa: Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote!⁷⁵

73 Na wachamngu watahimizwa kwenda Peponi kwa hishima makundi makundi, mpaka wakifika kwenye milango yake, wataambiwa na walinzi wake: Amani kubwa juu yenu! Mmet'ahirika duniani na uchafu wa maasi, na mmet'ahirika Akhera katika nafsi zenu kwa neema mlizo zipata. Basi ingieni Peponi mliko jaaliwa kukaa milele. Kwani nyinyi mna neema zisio pita akilini.

74 Na wachamngu watasema: Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu peke yake, ambaye ametutimizia aliyo tuahidi kwa ndimi za Mitume wake, na akatumilikisha ardhi ya Peponi tunashukia tutakapo humo. Ama hakika bora ya ujira wa wenye kutenda mema ni Pepo.

75 Na utaona, ewe mwenye kuona, Malaika wakiizunguka A'rshi, wakimtakasa Mwenyezi Mungu na kila upungufu, kwa utakaso unao fuatana na kumhimidi Muumba wao na Mlezi wao, na akapambanua baina ya viumbe vyote kwa uadilifu, na ulimwengu wote ukatamka kwa kusema: Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.

Sura 40 - Ghaafir (Al-Muumin)

Utangulizi

Sura hii imeanzia, kama zilivyo anzia Sura nyingi, kwa harufi mbili katika harufi za Alifbete. Na ikaanza kwa kutaja shani ya Qur'ani iliyo teremka kutokana na Mwenye nguvu, Mwenye ujuzi, Mwenye kusamehe madhambi, Mwenye kukubali toba, Mkali wa kuadhibu, Mwenye ukarimu. Kisha ikaitia Tawhidi, Imani ya Mwenyezi Mungu Mmoja, na kuacha kudanganyika na utawala ambao huenda makafiri wakawa nao, na ikawataka watu wakumbuke matokeo ya kaumu zilizo kuwa kabla yao.

Baada ya hayo Sura imesimulia khabari za wabebaji A'rshi, na kusabihi kwao, na madua yao. Na ikaeleza hali ya makafiri, na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu juu yao. Na Sura ikasimulia zaidi kuliko mara moja juu ya Ishara za Mwenyezi Mungu na uwezo wake katika nafsi zao, na yaliyo wazunguka ya mbinguni na kwenye ardhi, na neema zinazo wamiminikia, kama inavyo waitia katika zaidi kuliko Aya moja wamuamini Mwenyezi Mungu Mmoja kwa kumuabudu Yeye tu: "Basi mwombeni Mwenyezi Mungu mkimsafia Dini Yeye tu." "Na alisema Mola wenu Mlezi: Niombeni, nitakuitikieni!" "Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi Mungu, Muumba wa kila kitu. Hapana mungu isipo kuwa Yeye." Kama vile vile Sura hii ilivyo kusanya katika baadhi ya Aya zake maneno ya kukumbusha Siku ya Mwisho: "Na waonye siku inayo kurubia, wakati nyoyo zitakapo fika kooni nao wamejaa huzuni." Na Sura imesimulia kidogo katika kisa cha Musa a.s. pamoja na Firauni, na khasa walio amini katika watu wa Firauni. Na Sura ikakhitimishia kwa kuwataka watu watembe katika ardhi waone yaliyo wafika kaumu zilizo kuwako kabla yao, na vipi ulikuwa mwisho wa ghururi zao kwa ilimu walizo kuwa nazo. Na ilipo wafikia adhabu ya Mwenyezi Mungu walisema: Tunamuamini Mwenyezi Mungu pekee, na tunawakanya hao miungu tuliyo kuwa tukimshirikisha nao. Lakini hao wameamini baada ya kwisha pita wakati, "Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa wakati ambao wamekwisha iona adhabu yetu." Na huo ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe vyake, wala hutakuta mabadiliko katika mwendo wa Mwenyezi Mungu. Na inapo shuka adhabu hapo ndipo watapo khasiri makafiri.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. H'a, Mim.¹

2. Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu, Mwenye kujua.²

1 H'a, Mim, (H.M.) Harufi mbili katika harufi za Alifbete zinazo anzia Sura hii kwa mpango wa Qur'ani katika baadhi ya Sura, kuashiria kwamba hii Qur'ani imeundwa na maneno hayo hayo wanayo yatumia wanaadamu. Nayo juu ya hivyo imewashinda kuleta mfano wake.

2 Hii Qur'ani imeteremshwa kutokana na Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye kushinda, Mwenye kuvizunguka vitu vyote kwa ujuzi wake, naye ni Mwenye kupokea toba ya wenye kutubia, na Mkali wa kuadhibu, Mwenye neema nyingi; hapana wa kuabudiwa kwa haki isipo kuwa Yeye peke yake. Ni kwake Yeye peke yake ndio marejeo na mafikio.

3. Anaye samehe dhambi na anaye pokea toba, Mkali wa kuadhibu, Mwenye ukarimu, hakuna mungu ila Yeye; marejeo ni kwake.³
4. Hawazibishi Ishara za Mwenyezi Mungu ila walio kufuru; basi kusikughuri wewe kutanga tanga kwao katika nchi.⁴
5. Kabla yao walikadhibisha kaumu ya Nuhu na makundi mengine baada yao. Na kila taifa lilikuwa na hamu juu ya Mtume wao wamkamate. Na walibishana kwa upotovu ili kuipindua haki. Kwa hivyo niliwakamata. Basi ilikuwaje adhabu yangu!⁵
6. Namna hivi limewathibitikia makafiri neno la Mola wako Mlezi ya kwamba wao ni watu wa Motoni.⁶
7. Wale wanao beba A'rshi, na wanao izunguka, wanamsabihi na kumhimidi Mola wao Mlezi, na wanamuamini, na wanawaombea msamaha walio amini kwa kusema: Mola wetu Mlezi! Umekienea kila kitu kwa rehema na ujuzi. Basi wasamehe walio tubu na wakaifuata Njia yako, na waepushe na adhabu ya Jahannamu.⁷
8. Mola wetu Mlezi! Na waingize katika Bustani za Milele ulizo waahidi. Na uwape haya pia wale walio fanya mema miongoni mwa wazee wao na wake zao na dhuriya zao. Hakika Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.⁸
9. Na waepushe na maovu; kwani umwepushaye maovu siku hiyo, hakika umemrehemu; na huko ndiko kufuzu kukubwa.⁹
10. Kwa hakika wale walio kufuru watanadiwa: Bila ya shaka kukuchukieni Mwenyezi Mungu ni kukubwa kuliko kujichukia nyinyi nafsi zenu, mlipo kuwa mnaitwa kwenye Imani nanyi mkakataa.¹⁰
11. Watasema: Mola wetu Mlezi! Umetufisha mara mbili, na umetuhuisha mara mbili!

3 Tazama tanbihi ya 2.

4 Hawazibishi Ishara za Mwenyezi Mungu zenye kuonyesha dalili zake ila walio makafiri. Basi yasikukhadai huko kutanga tanga kwao katika nchi ukadhani kuwa Mwenyezi Mungu kawasahilishia mambo yao juu ya ukafiri wao.

5 Kabla ya hawa walikufuru kaumu ya Nuhu, na makundi mengine yaliyo jumuika kuwapinga Mitume baada ya kaumu yake Nuhu. Na hao wakawa na pupa ya kumletea shari Mtume wao wamtie nguvuni, na wakawa wanajadiliana katika upotovu usio kuwa na ukweli wowote, ili kwa upinzani wao wapate kuipindua haki iliyo kwisha thibiti. Basi Mimi nikawashika, nikawatia katika adhabu ya kuwang'olea mbali. Hebu angalia ilikuwaje adhabu yangu juu yao.

6 Na kila lilipo thibiti neno la adhabu juu ya mataifa yaliyo wakadhibisha Manabii wao, basi kadhaalika lilithibiti neno la Mola wako Mlezi juu ya hao wanao kukanusha wewe, ewe Muhammad, kwani hao ni watu wa Motoni, kwa kuwa wamekhiari ukafiri kuliko Imani.

7 Malaika wanao beba A'rshi, na wenye kuizunguka, wanamtakasa Mwenye kumiliki mambo yao na Mlezi wao, wanamtakasa kutokana na kila upungufu, kwa mtakaso ulio lingana na sifa zake. Na wanamuamini, na wanamwomba maghfira awaghufirie Waumini, huku wakisema: Ewe Mola wetu Mlezi! Rehema yako imeenea kila kitu, na Ujuzi wako umezunguka kila kitu, basi yasamehe makosa ya walio rejea kwako, na wakaifuata Njia yako, na waepushe na adhabu ya Motoni.

8 Na Malaika hawa husema: Ewe Mola wetu Mlezi! Waingize Waumini katika Mabustani ya Milele ulio waahidi kwa ndimi za Mitume wako, na pia waingize pamoja nao walio wema katika wazazi wao, na wake zao, na dhuriya zao. Hakika wewe peke yako ndiye Mwenye kushinda, wala hushindiki; Mwenye hikima usiye kosa.

9 Na husema katika dua zao: Waepushe Waumini malipo ya madhambi yao, na unaye muepusha Wewe na malipo ya madhambi yake Siku ya Malipo basi hakika ndio umemrehemu kwa fadhila yako. Kuepushwa na malipo ya madhambi ndio ushindi ulio fikilia ukomo mkubwa mno.

10 Hakika walio kufuru watanadiwa waambiwe: Bila ya shaka chuki ya Mwenyezi Mungu na bughdha yake kwenu ni kubwa kuliko chuki zenu wenyewe zilizo kupelekeeni mkapata adhabu pale mlipo itiwa kwenda kwenye Imani mara kwa mara nanyi mkakimbilia kwenye ukafiri.

Basi tunakiri madhambi yetu. Basi je, ipo njia ya kutoka?¹¹

12. Hayo ni hivyo kwa sababu mlikuwa akiombwa Mwenyezi Mungu peke yake mnakataa. Na akishirikishwa mnaamini. Basi hukumu ni ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Mkuu.¹²

13. Yeye ndiye anaye kuonyesheni Ishara zake, na anakuteremshieni kutoka mbinguni riziki. Na hapana anaye kumbuka ila anaye rejea.¹³

14. Basi mwombeni Mwenyezi Mungu mkimsafia Dini Yeye tu, na wangachukia makafiri.¹⁴

15. Yeye ndiye Mwenye vyeo vya juu, Mwenye A'rshi. Hupeleka Roho kwa amri yake juu ya amtakaye katika waja wake, ili kuonya kwa Siku ya Mkutano.¹⁵

16. Siku watakayo dhihiri wao. Hapana kitacho fichikana chochote chao kwa Mwenyezi Mungu. Ufalme ni wa nani leo? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mtenda nguvu.¹⁶

17. Leo kila nafsi italipwa kwa iliyo chuma. Hapana dhulma leo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.¹⁷

18. Na waonye siku inayo kurubia, wakati nyoyo zitakapo fika kooni, nao wamejaa huzuni. Madhaalimu hawatakuwa na rafiki, wala mwombezi wa kuitikiwa.¹⁸

19. (Mwenyezi Mungu) anajua khiyana ya macho na yanayo ficha vifua.¹⁹

20. Na Mwenyezi Mungu huhukumu kwa haki; lakini hao wanao waomba badala yake hawahukumu chochote. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia Mwenye kuona.²⁰

11 Makafiri watasema: Mola wetu Mlezi! Umetufishe vifo viwili, kifo kimoja katika uhai wetu wa duniani, na kifo kingine katika uhai wetu wa Barzakh, yaani kaburini. Na ukatuhisha mara mbili, mara moja ndiyo ya uhai wetu wa duniani, na mara ya pili ni wakati wa kufufuliwa kutoka makaburini. Basi, hebu, ipo njia ya kutoka kwetu kwenye adhabu. (*Tazama Maelezo 40:11*)

12 Hiyo ni adhabu mliyo nayo. Kwani mwendo wenu duniani ni kuwa akitajwa Mwenyezi Mungu peke yake nyinyi mnakufuru, na pindi akishirikishwa na mwinginewe ndio mnaamini. Na ikiwa huu ndio mwendo wenu basi mnastahiki kweli malipo ya ushirikina wenu. Basi hukumu ni ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Mkuu ambaye humlipa aliye kufuru kwa anavyo stahiki.

13 Mwenyezi Mungu ambaye anakuonyesheni dalili za uweza wake, basi anakuteremshieni kwa maslaha yenu maji kutoka mbinguni ambayo ni sababu ya riziki zenu. Na hapana anaye waidhika kwa haya ila mwenye kurejea akazifikiria Ishara za Mwenyezi Mungu.

14 Basi muabuduni Mwenyezi Mungu mkimsafia Yeye ibada, na hata walau wakiichukia makafiri ibada yenu na ikhlasi yenu.

15 Mwenyezi Mungu, Mwenye vyeo vya juu, Mwenye A'rshi, huteremsha Wahyi kwa hukumu yake na amri yake juu ya anaye mteuwa katika waja wake, ili awaonye watu adhabu ya kwenda kinyume na Mitume Siku ya kukutana viumbe vyote, Siku ya Hisabu watapo tokeza watu wazi, hapana lifichikanalo kwa Mwenyezi Mungu, watakuwa wakijisikilizanisha wao kwa wao wito unao tisha: Ufalme wa nani leo? Na jawabu ya kukata: Wa Mwenyezi Mungu, Mmoja, Mwenye kutengeka kwa hikima, Aliye pita mipaka kwa nguvu zake.

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Leo tunailipa kila nafsi kwa iliyo tenda. Hapana dhulma leo kwa kupunguziwa ujira au kuzidishiwa mateso. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi kuhisabu kwake, basi hachelewi na wakati wake.

18 Ewe Muhammad! Waonye, Siku ya Kiyama ipo karibu. Siku zitakapo kuwa nyoyo zipo kooni kwa wingi wa khofu, zimejaa majonzi, haziwezi hata kuyaelezea. Walio jidhulumu nafsi zao kwa ukafiri hawatakuwa na jamaa wala mwombezi wa kuwat'ii katika amri yao.

19. Na Yeye *Subhanahu* analijua jicho linalo khuni, na siri zilizo fichikana vifuani.

20 Na Mwenyezi Mungu anahukumu kwa uadilifu, na hao miungu ya uwongo wanayo iomba badala ya Mwenyezi Mungu haihukumu chochote, kwa kuwa haiwezi kitu. Hakika Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kuvizunguka vyote vinavyo sikia na vinavyo ona.

- 21.** Kwani hawatembe katika ardhi wakaona jinsi ulivyo kuwa mwisho wa walio kuwa kabla yao? Hao walikuwa wamewazidi hawa kwa nguvu na athari katika nchi. Na Mwenyezi Mungu aliwatia mkononi kwa sababu ya madhambi yao. Na wala hapakuwa wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu.²¹
- 22.** Hayo ni kwa sababu walikuwa wanawajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi, lakini wakawakataa, ndipo Mwenyezi Mungu akawakamata. Bila ya shaka Yeye ni Mwenye nguvu, Mkali wa kuadhibu.²²
- 23.** Na kwa yakini tulimtuma Musa pamoja na Ishara zetu na uthibitisho ulio wazi,²³
- 24.** Kumwendea Firauni na Hamana na Qaruni, wakasema: Huyu ni mchawi, mwongo mkubwa.²⁴
- 25.** Basi alipo waletea Haki inayo toka kwetu, walisema: Waueni watoto wanaume wa wale walio muamini na wawacheni hai wanawake wao. Na haviwi vitimbi vya makafiri ila katika upotovu.²⁵
- 26.** Na Firauni akasema: Niachieni nimuuwe Musa, naye amwite Mola wake Mlezi! Mimi nachelea asije kubadilishieni dini yenu, au akatangaza uharibifu katika nchi.²⁶
- 27.** Na Musa akasema: Mimi najikinga kwa Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi anilinde na kila mwenye jeuri asiye iamini Siku ya Hisabu.²⁷
- 28.** Na akasema mtu mmoja Muumini, aliye kuwa mmoja katika watu wa Firauni aliye ficha Imani yake: Mtamuwa mtu kwa sababu anasema Mola wangu Mlezi ni Mwenyezi Mungu? Na hali naye amekujieni na hoja zilizo wazi? Na akiwa yeye mwongo basi uwongo wake ni juu yake mwenyewe, na akiwa mkweli yatakufikieni baadhi ya hayo anayo kuahidini. Hakika Mwenyezi Mungu hamwongoi apindukiaye mipaka, mwongo mkubwa.²⁸

21 Kwani hao washirikina wamekaa kitako tu wala hawatembe katika ardhi wakaona vipi ilikuwa hali ya mataifa yaliyo kuwa kabla yao? Walikuwa wana nguvu kuliko wao na walijenga zaidi kuliko hawa, nao Mwenyezi Mungu aliwang'olea mbali kwa madhambi yao, wala hawakuwa na mlinzi wa kuwalinda na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

22 Na adhabu hiyo iliwatremkia kwa sababu ilikuwa Watume wao wakiwajia na dalili zilizo wazi, nao wakazikataa, basi Mwenyezi Mungu akafanya haraka kuwapelekea adhabu ya kuwang'oa. Hakika Yeye ana nguvu kubwa mno, na amefikilia ukomo katika kuadhibu.

23 Ninaapa kuwa tulimtuma Musa na miujiza yetu na ushahidi wenye uthibitisho ulio wazi kumpelekea Firauni na Hamana na Qaruni, wakasema: Huyu ni mchawi kwa hiyo anayo dai kuwa ni miujiza, na amepita mipaka kwa uwongo katika madai yake kuwa yeye ni Mtume aliye toka kwa Mola wake Mlezi!
24 Tazama tanbihi ya 23.

25 Musa alipo waletea Haki kutoka kwetu, Firauni na wafuasi wake walio kuwa pamoja naye walisema: Wauweni watoto wa kiume wa hao walio amini pamoja naye, na waachilieni wahai binti zao! Na vitimbi vya makafiri haiwi ila kuondoka, na kuangamia, na kupotea.

26 Na Firauni akasema: Nachilieni nimuuwe Musa, naye naamwite huyo Mola wake Mlezi amwokoe kwangu! Hakika mimi nakhofia asije huyu akaigeuza dini yenu, enyi watu wangu, au akaeneza fitna katika nchi.

27 Na Musa akamwambia Firauni na watu wake: Hakika mimi nimejilinda na Mwenye kumiliki mambo yangu ambaye ndiye aliye nilea, na ndiye Mwenye kumiliki mambo yenu pia, na Mwenye kukuleeni nyinyi kwa neema zake na hisani zake, nimejilinda na kila anaye jivuna na kutakabari, asiye iamini Siku ya Hisabu.

28 Akasema mtu mmoja Muumini anaye ficha Imani yake katika watu wa Firauni, akiwasemeza watu wake: Mnataka kumuwa mtu kwa sababu anasema: Mungu wangu ninaye muabudu ni Mwenyezi Mungu, naye amekuleteni dalili zilizo wazi zinazo tokana na Mwenye kumiliki mambo yenu na Mlezi wenu? Na akiwa yeye mwongo, basi uwongo wake ni juu yake yeye peke yake, balaa ya uwongo wake itamwangukia mwenyewe. Na akiwa ni mkweli baadhi ya adhabu anazo tutahadharisha nazo zitakuteremkieni nyinyi.

- 29.** Enyi watu wangu! Leo mna ufalme, mmeshinda katika nchi; basi ni nani atakaye nisaidia kutuokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu kama ikitufikia? Firauni akasema: Sikupeni shauri ila ile niliyo iona, wala sikuongozeni ila kwenye njia ya uwongofu.²⁹
- 30.** Na akasema yule aliye amini: Enyi watu wangu! Hakika mimi nakukhofieni mfano wa siku za makundi,³⁰
- 31.** Mfano wa hali ya watu wa Nuhu na A'di na Thamudi na wale wa baada yao. Na Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu waja.³¹
- 32.** Na enyi watu wangu! Hakika mimi nakukhofieni Siku ya mayowe.³²
- 33.** Siku mtakapo geuka kurudi nyuma. Hamtakuwa na wa kukulindeneni kwa Mwenyezi Mungu. Na mwenye kuhukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi huyo hana wa kumwongoa.³³
- 34.** Na alikwisha wajieni Yusuf zamani kwa dalili zilizo wazi, lakini nyinyi mliendelea katika shaka kwa yale aliyo kuleteeni; mpaka alipo kufa mkasema: Mwenyezi Mungu hataleta kabisa Mtume baada yake. Kama hivyo Mwenyezi Mungu humwacha kupotea anaye pindukia mipaka katika maasi anaye jitia shaka.³⁴
- 35.** Hao ambao wanajadiliana katika Ishara za Mwenyezi Mungu pasipo ushahidi wowote ulio wafikia, ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya walio amini. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu apigavyo muhuri juu ya kila moyo wa jeuri anaye jivuna.³⁵
- 36.** Na Firauni akasema: Ewe Hamana! Nijengee mnara ili nipate kuzifikia njia,³⁶
- 37.** Njia za mbinguni ili nikamwone Mungu wa Musa. Na kwa hakika mimi bila ya

Hakika Mwenyezi Mungu hamwafikishi njia ya uwokovu mwenye kupita mipaka, aliye mwongo mno..
29 Enyi watu wangu! Leo nyinyi mnao ufalme, na ni watu wa juu katika nchi ya Misri, wala hapana mwenginewe. Lakini ni nani atakaye kuingeni na adhabu ya Mwenyezi Mungu pindi ikitujia? Firauni akasema: Sikwambiini rai ila ambayo mimi mwenyewe ninayo itakidi. Na sikuongozeni kwa rai hii ila njia ya uwongofu.

30 Akasema yule mtu aliye amini katika watu wa Firauni: Enyi watu wangu! Hakika mimi nakukhofieni isikufikieni siku kama ile siku walipo jikusanya watu makundi mbali mbali kuwapinga Mtume wao, mfano wa ada ya kaumu Nuhu, na ya A'di, na ya Thamudi, na mataifa mengine yaliyo kuja baada yao. Wala Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu waja wake.

31 Tazama tanbihi ya 30.

32 Na enyi watu wangu! Mimi nakukhofieni siku viumbe watapo pigiana makelele, siku mtapo kimbia kurudi nyuma, hapana wa kukuingeni na Mwenyezi Mungu. Na mwenye kuachiliwa na Mwenyezi Mungu kupotea - kwa kuwa anamjua kuwa amekhiari upotovu kuliko uwongofu - basi hatokuwa na mwongozi wa kumwongoa.

33 Tazama tanbihi ua 32.

34 Ninaapa! Bila ya shaka alikwisha kujieni Yusuf na Ishara zilizo wazi. Nanyi hamkuacha kuwa na shaka na hayo aliyo kuja nayo kwenu, mpaka alipo kwisha kufa mkasema: Mwenyezi Mungu hatoleta tena Mtume mwengine baada ya Yusuf. Mfano wa upotovu kama huu mba ya Mwenyezi Mungu humwacha kupotea yule aliye pindukia mipaka, mwingi wa mashaka na wasiwasi.

35 Wanao bishana juu ya Ishara za Mwenyezi Mungu bila ushahidi wowote ulio wajia, humkirihisha mno na kumchukiza Mwenyezi Mungu na Waumini kwa yale majadiliano waliyo yatilia muhuri. Mfano wa muhuri huu Mwenyezi Mungu anaupiga juu ya kila moyo ulio takabari juu ya viumbe wenzake, na ukataka kuwatawala.

36 Na Firauni akasema: Ewe Hamana! Nijengee jengo refu nifikilie njia za mbinguni nipate kumwona huyo Mungu wa Musa. Na mimi nina hakika huyu ni mwongo kwa anavyo jidai kuwa yeye ati ni Mtume. Mfano wa pumbao la uwongo kama hivi Firauni alipambiwa uovu wa vitendo vyake, hata akaviona mwenyewe kuwa ni vizuri, na akazuilika na njia ya haki kwa kukhiari mwenyewe njia ya upotovu. Na havikuwa vitimbi vya Firauni ila katika upotovu tu.

shaka namjua kuwa ni mwongo tu. Na hivi ndivyo Firauni alivyo pambiwa ubaya wa vitendo vyake, na akazuiliwa Njia. Na vitimbi vya Firauni havikuwa ila katika kuangamia tu.³⁷

38. Na yule aliye amini alisema: Enyi watu wangu! Nifuateni mimi, nitakuongozeni njia ya uwongozi mwema.³⁸

39. Enyi watu wangu! Hakika haya maisha ya dunia ni starehe ipitayo tu, na hakika Akhera ndiyo nyumba ya daima.³⁹

40. Mwenye kutenda uovu hatalipwa ila sawa na huo uwovu wake, na anaye tenda wema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini, basi hao wataingia Peponi, waruzukiwe humo bila ya hisabu.⁴⁰

41. Na enyi watu wangu! Kwa nini mimi nakuiteni kwenye uwokofu, nanyi mnaniita kwenye Moto?⁴¹

42. Mnaniita nimkufuru Mwenyezi Mungu na nimshirikishe na yule ambaye simjui, nami nakuiteni kwa Mwenye nguvu Mwenye kusamehe?⁴²

43. Bila ya shaka mnaye niitia kumuabudu hastahiki wito duniani wala Akhera. Na hakika marejeo yetu ni kwa Mwenyezi Mungu. Na wanao pindukia mipaka ndio watu wa Motoni!⁴³

44. Basi mtayakumbuka ninayo kuambieni. Nami namkabidhi Mwenyezi Mungu mambo yangu. Hakika Mwenyezi Mungu anawaona waja wake.⁴⁴

45. Basi Mwenyezi Mungu akamlinda na ubaya wa hila walizo zifanya. Na adhabu mbaya itawazunguka watu wa Firauni.⁴⁵

46. Wanaonyeshwa Moto asubuhi na jioni. Na itapo fika Saa ya Kiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!⁴⁶

47. Na watapo hojiana huko Motoni, wanyonge watawaambia walio jitukuza: Hakika

37 Tazama tanbihi ya 36.

38 Na akasema yule aliye amini katika watu wa Firauni: Enyi watu wangu! Nifuateni mimi, nitakuongozeni njia njema!

39 Enyi watu wangu! Haya maisha ya duniani si chochote ila ni kama starehe ya muda ya mwenye kupanda kipando, inakwisha upesi. Na makaazi ya Akhera, hayo tu peke yake, ndiyo makaazi ya kudumu.

40 Mwenye kutenda uovu duniani hatolipwa kwa uovu huo huko Akhera ila kwa mfano wake. Na mwenye kutenda wema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini, basi hao wataingia Peponi watakapo ruzukiwa bila ya kipimo cha kuhisabiwa na wenye kuhisabu.

41 Na enyi watu wangu! Kwani mimi nina nini? Mimi nakuiteni mfuate njia za kuokoka, na nyinyi mnaniita niingie Motoni! Mnaniita nimkufuru Mwenyezi Mungu kwa kumshirikisha Yeye na vitu nisivyo vijua, na hali mimi nakuitieni mwende kwa Mwenye Nguvu asiye shindwa, Mwingi wa kusamehe madhambi!

42 Tazama tanbihi 41.

43 Bila ya shaka yoyote huyo mungu mnaye niitia nimuabudu hana wito wowote unao stahiki kuitikiwa la duniani wala Akhera. Na hakika marejeo yetu sote ni kwa Mwenyezi Mungu, na wenye kupita mipaka ndio watu wa Motoni, wala si Waumini walio kaa sawa.

44 Basi watakuja jua ukweli wa niliyo kuambieni, na mimi namtegemezea mambo yangu Mwenyezi Mungu. Hakika jicho la Mwenyezi Mungu limewaenea waja wake wote, na Yeye ni Mwenye kuwalipa kwa vitendo vyao.

45 Mwenyezi Mungu akamlinda yule Muumini katika watu wa Firauni mateso ya vitimbi vyao, na ikawazunguka watu wa Firauni adhabu mbaya, nayo ni Moto wanao uingia asubuhi na jioni. Haya ni ya duniani na wapo katika ulimwengu wa Barzakh, kaburini. Na Siku ya Kiyama, atasema Mwenyezi Mungu: Waingizeni watu wa Firauni kwenye adhabu iliyo kali kabisa!

46 Tazama tanbihi ya 45.

sisi tulikuwa wafuasi wenu, basi je, hamtuondolei sehemu ya huu Moto?⁴⁷

48. Watasema walio jitukuza: Hakika sote sisi tumo humo humo! Kwani Mwenyezi Mungu kesho hukumu baina ya waja!⁴⁸

49. Na walio Motoni watawaambia walinzi wa Jahannamu: Mwombeni Mola wenu Mlezi atupunguzie walau siku moja ya adhabu.⁴⁹

50. Nao watasema: Je! Hawakuwa wakikufikieni Mitume wenu kwa hoja zilizo wazi? Watasema: Kwani? Watasema: Basi ombeni! Na maombi ya makafiri hayawi ila ni kupotea bure.⁵⁰

51. Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watapo simama Mashahidi,⁵¹

52. Siku ambayo hautawafaa madhaalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata makaazi mabaya kabisa.⁵²

53. Na kwa hakika tulimpa Musa uwongofu, na tukawarithisha Wana wa Israili Kitabu,⁵³

54. Ambacho ni Uwongofu na Ukumbusho kwa wenye akili.⁵⁴

55. Basi subiri. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Na omba msamaha kwa dhambi zako, na umtakase Mola wako Mlezi kwa kumhimidi jioni na asubuhi.⁵⁵

56. Hakika hao wanao bishana katika Ishara za Mwenyezi Mungu bila ya uthibitisho wowote uliyo wajia, hawana vifua ni mwao ila kutaka ukubwa tu, na wala huo hawaufikilii. Basi jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.⁵⁶

47 Ewe Muhammad! Watajie pale wanapo zozana watu wa Motoni humo, wakawa walio kuwa wanyonge, nao ni wafuasi, wakiwaambia wanao takabari, nao ni maraisi: “Sisi tulikuwa duniani ni wafuasi wenu, basi je, hamtuchukulii baadhi ya adhabu ya moto?”

48 Na walio takabari waseme: “Hakika sote sisi tumo humo, sisi na nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu amehukumu kwa haki baina ya waja. Basi kila mmoja wetu amepata adhabu aliyo hukumiwa juu yake.”

49 Watasema walio Motoni, wanyonge na wakuu, kuwaambia walinzi wa Jahannamu wakiwaomba msaada: Muombeni Mungu wenu atupunguzie japo siku moja tupumzike na adhabu.

50 Walinzi wa Jahannamu watawaambia kwa kuwahizi: Kwani hamkunabihika kwa yaliyo kuwa mkiteremshiwa, na hali walikuwa wakikujieni Mitume na ushahidi ulio wazi? Na watasema watu wa Motoni: Kwani? Walitujia Mitume na sisi tukawakadhibisha. Walinzi wakasema: Ikiwa mambo ni hivyo, basi waombeni nyinyi! Lakini madua ya makafiri hayana ila kupotea bure.

51 Hakika Sisi bila ya shaka tunawanusuru Mitume wetu na Waumini katika maisha ya duniani kwa kulipiza juu ya maadui wao, na kusimamisha hoja juu yao; na Siku ya Kiyama watasimama Mashahidi washuhudie kwamba Mitume wamefikisha Ujumbe wao, na washuhudie kwamba makafiri waliukadhibisha.

52 Siku ambayo madhaalimu hautawafaa udhuru wao kwa yale waliyo yakosa kuyatenda duniani. Nao watapata laana, yaani watafukuzwa kwenye rehema, na watapata makaazi maovu kabisa.

53 Naapa kwamba tulimpa Musa cha kuongoa kwendea Haki, na tukawarithisha Wana wa Israili Taurati yenye kuongoa na yenye kuwakumbusha wenye akili zilizo nzima.

54 Tazama tanbihi ya 53.

55 Ikiwa umejua tuliyoy kusimulia, basi subiri, ewe Muhammad, kwa maudhi yanayo kupata. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kukunusuru wewe na kuwanusuru Waumini ni kweli isiyoy geuka. Na taka maghfira kutoka kwa Mola wako Mlezi kwa hayo ambayo kwa mnasaba wako wewe huhisabiwa kuwa ni dhambi. Na mtakase Mola wako Mlezi na kila upungufu kwa mtakaso unao ambatana na kumsifu jioni na asubuhi.

56 Hakika hao wanao jadili katika dalili za Mwenyezi Mungu bila ya hoja iliyo tokana naye Yeye Mtukufu, hamna vifua ni mwao ila kutaka uluwa, ubora, wasiifuatate Haki, wala huko kutaka kwao uluwa, ubora, hakuwafikishii walitakalo. Basi wewe iombe Hifadhi kutokana na Mwenyezi Mungu; kwani Yeye hakika ni Mwenye kuenea kila kitu kusikia kwake na kuona kwake.

57. Bila ya shaka kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.⁵⁷
58. Na kipofu na mwenye kuona hawalingani; na walio amini na watendao mema hawalingani na muovu. Ni machache mnayo yakumbuka.⁵⁸
59. Hakika Saa (ya Kiyama) itafika, nayo haina shaka. Lakini watu wengi hawaamini.⁵⁹
60. Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni. Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike.⁶⁰
61. Mwenyezi Mungu aliye kufanyieni usiku ili mpate kutulia humo, na mchana wa kuonea. Hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mwenye fadhila juu ya watu, lakini watu wengi hawashukuru.⁶¹
62. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi, Muumba wa kila kitu. Hapana mungu ila Yeye; basi mnageuzwa wapi?⁶²
63. Namna hivi ndivyo walivyo geuzwa walio kuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu.⁶³
64. Ni Mwenyezi Mungu aliye kufanyieni ardhi kuwa ni pahala pa kukaa, na mbingu kuwa dari. Na akakutieni sura, na akazifanya nzuri sura zenu, na akakuruzukuni vitu vizuri. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁶⁴
65. Yeye ndiye aliye Hai - hapana mungu isipo kuwa Yeye. Basi muabuduni Yeye mkimsafishia Dini Yeye. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁶⁵
66. Sema: Mimi nimekatazwa kuwaabudu hao mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, zilipo nijia hoja zilizo dhaahiri kutokana na Mola wangu Mlezi. Na

57 Ninaapa: Bila ya shaka kuziumba mbingu na ardhi ni jambo kubwa zaidi kuliko kuwaumba watu. Lakini wengi wa watu wameitupa ilimu, wakawa hawaamini kufufuliwa juu ya kukubali kwao kwamba Yeye ndiye Muumba mbingu na ardhi.

58 Na hawawi sawa, kipofu asiyo iona Haki, na mwenye kuijua. Wala hawawi sawa wema wenye kuamini na wakatenda mema, na muovu wa itikadi na vitendo. Ni kwa uchache, uchache mno, ndio mnakumbuka, enyi watu!

59 Hakika Kiyama kitakuja tu, hapana shaka yoyote. Na lakini wengi wa watu hawasadiki.

60 Na anasema Muumba wenu na Mwenye kumiliki mambo yenu yote: Niombeni nami nitakupeni! Hakika wale wanao takabari hata wakakataa kuniomba wataingia Jahannamu nao ni madhalili wanyonge.

61 Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye kujaalieni usiku mpate kutua ndani yake mpumzike na kazi, na mchana wenye mwangaza mpate kufanya kazi ndani yake. Hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mwenye fadhila kuu juu ya watu. Lakini watu wengi hawamshukuru juu ya neema zake.

62 Huyu Mwenye kukunee mesheni kwa neema hizi tukufu ndiye Mwenyezi Mungu, Mwenye kumiliki mambo yenu, Muumba wa kila kitu, hapana wa kuabudiwa kwa haki ila Yeye. Basi mtaelekea wapi kwa ibada mkimwacha Yeye?

63 Mfano wa kukengeuka huku kuiacha Haki kuendea upotovu, walikengeuka walio kuwa kabla yenu. Wakazikanya Ishara za Mwenyezi Mungu na wakazikataa.

64 Ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye kufanyieni ardhi iwe ni pahala panapo silihi maisha yenu, na mbingu zikawa ni jengo lilio shikamana. Na akakadiria kukuumbeni nyinyi, akazitengeneza sura zenu, na akakujaalieni na umbo zuri lilio nyooka. Na akakuruzukuni katika vitu vya halali mnavyo viona vitamu. Mneemesha huyo kwa neema hizi ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mwenye kumiliki ulimwengu wote, na Mwenye kuulea.

65 Yeye pekee Mwenye uhai wa daima dawamu, hapana wa kuabudiwa kwa Haki ila Yeye. Basi muelekeeni Yeye kwa kumuomba, mkimsafia ibada Yeye. Sifa njema zote ni haki iliyo thibiti kwa Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe vyote.

nimeamrisha nisilimu kwa Mola wa walimwengu wote.⁶⁶

67. Yeye ndiye aliye kuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu, kisha akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha mpate kufikilia utu uzima, kisha mpate kuwa wazee. Na kati yenu wapo wanao kufa kabla, na ili mfikie muda ulio kwisha wekwa, na ili mpate kufahamu.⁶⁷

68. Yeye ndiye anaye huisha na anaye fisha. Akihukumu jambo liwe, basi huliambia: Kuwa! Likawa.⁶⁸

69. Je! Huwaoni wale wanao bishana katika Ishara za Mwenyezi Mungu? Wanageuziwa wapi?⁶⁹

70. Ambao wamekanusha Kitabu na yale tuliyo watuma Mitume wetu. Basi watakuja jua.⁷⁰

71. Zitakapo kuwa pingu shingoni mwao na minyororo, huku wanabururwa⁷¹

72. Katika maji ya moto, kisha wanaunguzwa Motoni,⁷²

73. Tena wataambiwa: Wako wapi mlio kuwa mkiwashirikisha⁷³

74. Badala ya Mwenyezi Mungu? Watasema: Wametupotea, bali tangu zamani hatukuwa tukiomba kitu! Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anawaachia makafiri wapotelee mbali.⁷⁴

75. Haya ni kwa sababu mlikuwa mkijitapa katika ardhi pasipo haki, na kwa sababu mlikuwa mkijishaua.⁷⁵

66 Ewe Mtume! Sema: Hakika mimi nimekatazwa kuiabudu miungu mnayo iabudu nyinyi badala ya Mwenyezi Mungu, zilipo nijia hoja kutoka kwa Mola wangu Mlezi, na nikaamrisha nimfuate Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote katika mambo yangu yote.

67 Mwenyezi Mungu, peke yake, ndiye aliye kuumbeni, eni wanaadamu, kutokana na udongo, kisha akaageza udongo ukawa tone la manii, kisha akalifanya tone la manii kuwa pande la damu iliyo gandana, kisha akakutoeni kwenye matumbo ya mama zenu kuwa ni watoto wachanga. Kisha akaukuza umri wenu mpaka mkakamilika nguvu zenu na akili, tena ukawa mrefu umri wenu mpaka mkawa wazee. Na wako kati yenu wanao kufa kabla ya kufikia ujana au uzee. Na Mwenyezi Mungu akakuumbeni kwa namna hii ili mfikilie wakati maalumu kwake Yeye, nao ni wakati wa kufufuliwa; na kwa ajili mpate kupima na kufahamu hikima na mazingatio katika mageuzi haya. (*Tazama Maelezo 40:67*)

68 Mwenyezi Mungu ndiye anaye huisha na kufisha. Akitaka jambo lolote kulidhihirisha katika kuwepo basi huliambia: Kuwa! Na huwa bila ya taakhira.

69 Je! Huwaangalii hao wanao zozana katika Ishara za Mwenyezi Mungu zilizo wazi, vipi walivyo geuzwa nadhari yao katika hizo, na wanaendelea kushikilia ule ule upotovu wao walio nao?

70 Walio ikadhibisha Qur'ani na Ujumbe tulio watumia Mitume wetu, Ufunuo wote, watakuja jua matokeo ya kukanusha kwao zitapo kuwa pingu na minyororo zipo shingoni mwao, wakibururwa kwazo katika maji yaliyo fikia ukomo wa moto, tena baadae watupwe Motoni waokwe kwenye joto lake. Kisha waambiwe kwa kuwakejeli na kuwahizi: Wako wapi hao miungu yenu mliyo kuwa mkiiabudu badala ya Mwenyezi Mungu? Watasema makafiri: Wametupotea. Bali kwa hakika sisi hatukuwa hapo zamani duniani tukiabudu chochote. Katika mfano wa upotovu mbaya kama huu ndio Mwenyezi Mungu anawawacha makafiri waipotee Njia ya Haki kwa kujua kwake kwamba hao wamekhiari upotovu kuliko uwongofu.

71 Tazama tanbihi ya 70.

72 Tazama tanbihi ya 70.

73 Tazama tanbihi ya 70.

74 Tazama tanbihi ya 70.

75 Makafiri wataambiwa: Adhabu hiyo ni kwa sababu ya mlivyo kuwa katika dunia mkifurahi katika nchi kwa jambo lisilo stahiki kufurahikiwa, na kwa sababu ya kufurahikia kwenu kwa maudhi yaliyo kuwa yakiwasibu Manabii wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake. Basi ingieni kwenye milango ya Jahannamu, ambako mmekadiriwa mkae daima dawamu. Pahala paovu kabisa pa kukaa wenye kujivuna ni Jahannamu.

- 76.** Ingieni kwenye milango ya Jahannamu, mdumu humo milele. Basi ni maovu yaliyoje makaazi ya wanao takabari!⁷⁶
- 77.** Basi subiri, hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Na ama tukikuonyesha baadhi ya yale tuliyo waahidi au tukikufisha, lakini wao watarudishwa kwetu tu.⁷⁷
- 78.** Na bila ya shaka tuliwatuma Mitume kabla yako. Wengine katika hao tumekusimulia khabari zao, na wengine hatukukusimulia. Na haiwi Mtume alete Ishara yoyote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Basi ikija amri ya Mwenyezi Mungu huhukumiwa kwa Haki, na hapo wapotofu watakhasiri.⁷⁸
- 79.** Mwenyezi Mungu aliye kujaalieni nyama hoa, mifugo, ili muwapande baadhi yao, na muwale baadhi yao.⁷⁹
- 80.** Na katika hao mnayo manufaa kadhaa wa kadhaa, na mnapata kwao haja ziliomo vifuani mwenu; na mnachukuliwa juu yao, na juu ya marikebu.⁸⁰
- 81.** Naye anakuonyesheni Ishara zake. Basi Ishara gani za Mwenyezi Mungu mnazo zikataa?⁸¹
- 82.** Kwani hawatembe katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa walio kuwa kabla yao? Wao walikuwa wengi kuliko hawa, na wamewashinda kwa nguvu na athari katika nchi. Wala hayakuwafaa hayo waliyo kuwa wakiyachuma.⁸²
- 83.** Walipo wajia Mitume wao kwa dalili zilizo wazi walijitapa kwa ilimu waliyo kuwa nayo. Basi yakawazunguka waliyo kuwa wakiyafanyia maskhara.⁸³
- 84.** Walipo iona adhabu yetu walisema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni wa pekee, na tunaikataa miungu tuliyo kuwa tukiishirikisha naye.⁸⁴

76 Tazama tanbihi ya 75.

77 Subiri, ewe Muhammad! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu kwako ya kwamba atawaadhibu maadui wako, ni kweli isiyo na shaka yoyote. Na adhabu itawafikia tu, ama wakati wa uhai wako au wakati watapo rejea wao kwetu! Wakiacha baadhi ya adhabu tunayo wahadharisha nayo katika uhai wako, basi. Na ikiwa tutakufisha, basi watarejea kwetu. Nasi tutawahisabia waliyo kuwa wakiyatenda.

78 Ninaapa: Bila ya shaka tuliwatuma Mitume wengi kabla yako wewe. Wengine tumekuzungumzia khabari zao, na wengine hatukukuzungumzia khabari zao. Wala haikuwa Mtume yeyote kuleta muujiza ila kwa apendavyo Mwenyezi Mungu na kutaka kwake. Hawezi kuleta kwa nafsi yake tu, wala kwa watakavyo watu wake. Na inapo kuja amri ya Mwenyezi Mungu ya kuleta adhabu duniani au Akhera wanahukumiwa kwa uadilifu. Na wakati huo wapotovu huwa ndio wenye kukhasiri.

79 Mwenyezi Mungu ndiye aliye kudhalilishieni ngamia, mpate kuwapanda wengine, na wengine muwale. 80 Na mnapata kwao manufaa mengi, mbali ya kuwapanda na kuwala; na ili mpate kufikilia haja zenu mnazo zishughulikia nafsi zenu, kama kuburura mizigo na kuibeba, na kadhaalika. Na juu ya ngamia, ambaye ni katika nyama hoa, na juu ya marikebu, mnajipakia nyinyi wenyewe na mizigo yenu.

81 Mwenyezi Mungu anakuonyesheni dalili zake, basi hebu nambieni dalili gani katika hizo mnazo zikataa? Na hizo dalili zenyewe ziwazi, hawezi kuzikataa yeyote mwenye akili hata kidogo.

82 Je! Kwani hao watu wamekaa tu, hawazunguki ulimwenguni wakaona ulikuwaje mwisho wa wale walio kuwa kabla yao, walivyo hilikishwa na wakaangamizwa? Hao walio kabla yao walikuwa wengi kwa kuwahisabu kuliko wao, na walikuwa na nguvu na waliathiri kwa majenzi na maendeleo kushinda wao. Hapana kilicho wakinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu katika hayo waliyo yachuma, si mali wala nguvu, wala utawala.

83 Basi Mitume wao walipo wajia mataifa haya kwa sharia na miujiza iliyo kuwa wazi, hayo mataifa yalifurahi na kujitapa kwa kuwa wao ati wana ilimu za dunia, na wakawafanyia maskhara Mitume. Ikawateremkia adhabu waliyo wakhubiria Mitume, na hali wao wakiwakejeli.

84 Mataifa haya yalipo ona adhabu imekuwa kali walisema: Tumemsadiki Mwenyezi Mungu pekee, na tumewakataa miungu ambao kwa sababu yao tulikuwa washirikina.

85. Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa kitu wakati ambao wamekwisha iona adhabu yetu. Huu ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu ulio kuwa kwa waja wake. Na hapo walio kufuru walikhasiri.⁸⁵

85 Imani yao haikuwafaa kitu wakati walipo kwisha ona ukali wa adhabu yetu. Mwenyezi Mungu alikwenda mwendo ule ule aliyo kuwa akienda nao waja wake, nao ni kutokukubali Imani wakati wa kuteremka adhabu. Na makafiri ndio walio khasiri wakati wa kuteremka adhabu.

Sura 41 - Fuss'ilat (H'a Mim Sajdah)

Utangulizi

Sura hii imeanzia kwa harufi mbili katika harufi za alifbete kama inavyo fanya Qur'ani katika Sura nyingi. Sura hii imeeleza katika nyingi ya Aya zake shani ya Qur'ani na mambo iliyo kusanya yaliyo khusu bishara na maonyo. Na imeeleza msimamo wa washirikina kukhusu Qur'ani, katika kuipuuza na kuupiga vita wito wake, na msimamo wa Mtume kwa mnasaba wa makafiri, kwa kusimama imara juu ya wito wake kwao na kuwaambia: “Hakika mimi ni mtu kama nyinyi; inafunuliwa kwangu ya kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Basi tengeneeni kumwendea Yeye, na mumtake msamaha.” Na Sura inaingilia kuwakumbusha washirikina uweza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kuziumba mbingu na ardhi, kisha inawahadharisha na yaliyo watokelea watu wa mataifa walio karibu mno na makwao, nao ni kina A'adi na Thamudi. Na inawakumbusha Siku ya Akhera, siku yatakapo washuhudia masikio yao, na macho yao, na ngozi zao, kwa waliyo kuwa wakiyatenda; na mijadiliano itakayo kuwa baina yao na viungo vyao siku hiyo; na watayo yaomba wafwasi kwa Mola wao Mlezi Siku ya Kiyama: “Mola wetu Mlezi! Tuonyeshe wale walio tupoteza miongoni mwa majini na watu ili tuwaweke chini ya miguu yetu, wapate kuwa miongoni mwa walio chini kabisa.” Na kama ilivyo kuwa mwendo wa Mwenyezi Mungu katika Kitabu hichi akisimulia khabari ya makafiri, husimulia pia khabari za Waumini. Basi Sura hii imesimulia khabari za walio sema: “Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu”, kisha wakasimama sawa sawa, neema za daima alizo waneemesha, na akalinganisha baina ya kheri na shari: “Wema haulingani na uovu”.

Kisha Sura inataka watu waangalie Ishara za uweza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu zinazo onyesha kumkinika kufufuliwa maiti, kisha inarejea tena kuzidi kuwakemea wanao zigeuza Aya za Mwenyezi Mungu, na kwamba hao hawamkhofu Mwenyezi Mungu. Na kwamba hakika Kitabu hichi hakiingiliwi na upotovu kutoka mbele yake wala nyuma yake. Huu ni mteremsho ulio tokana na Mwenye hikima, Msifika. Na hakika Ujumbe wa Muhammad si ujumbe ulio zuliwa tu.

Na Sura inathibitisha khulka moja katika khulka za binaadamu, nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu akimneemesha mtu huipuuza Haki, na ikimgusa tu shari anakuwa na madua marefu marefu.

Na Sura imekhitimisha kwa kuthibitisha mambo mawili muhimu kabisa, nayo ni la kwanza: kutaja kwa Qur'ani Tukufu yenyewe Haki iliyomo ndani yake isiyo na shaka yoyote: “Tutawaonyesha Aya zetu katika upeo wa macho na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli.” Na la pili lake kuwa hilo wanalo litegemea makafiri si lolote ila ni shaka tu ya kufufuliwa iliyo wapelekea kuwa nayo ukafiri na upotovu. “Ama hakika wao bado wamo katika shaka ya kukutana na Mola wao Mlezi. Hakika Yeye amekizunguka kila kitu.”

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. H'a Mim¹

2. Uteremsho huu umetoka kwa Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.²

3. Hichi ni Kitabu kilicho pambanuliwa Aya zake, cha kusomwa kwa Kiarabu kwa watu wanao jua.³

4. Kitoacho khabari njema, na chenye kuonya. Lakini wengi katika wao wamepuuza; kwa hivyo hawasikii.⁴

5. Na wakasema: Nyoyo zetu zimo katika vifuniko kwa hayo unayo tuitia, na masikio yetu yana uziwi, na baina yetu na wewe lipo pazia. Basi wewe tenda, nasi tunatenda.⁵

6. Sema: Hakika mimi ni mtu kama nyinyi; inafunuliwa kwangu ya kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Basi nyookeeni sawa kumwendea Yeye, na mumtake msamaha, na ole wao wanao mshirikisha,⁶

7. Ambao hawatoi Zaka na wanaikataa Akhera.⁷

8. Hakika wanao amini na wakatenda mema watakuwa na ujira usio na ukomo.⁸

9. Sema: Hivyo nyinyi mnamkataa aliye umba ardhi katika siku mbili, na mnamfanyia washirika? Huyu ndiye Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁹

10. Na akaweka humo milima juu yake, na akabarikia humo na akakadiria humo chakula chake katika siku nne. Haya ni sawa kabisa kwa wanao uliza.¹⁰

1 (H'a Mim) Hizi harufi mbili katika harufi za alifbete zililo fungulia Sura hii kama ilivyo ada ya Qur'ani katika Sura nyingi, ili kuzindua watu watanabahi, na pia kuonyesha dalili ya muujiza wa Qur'ani

2 Kitabu hichi ni mteremsho wa namna ya peke yake, kutokana na Mneemeshaji wa neema kubwa na neema ndogo.

3 Kitabu hichi ni namna ya peke yake kwa uzuri wake kwa matamshi na ibara yake ya utungaji, na kwa maana inavyo pambanua baina Haki na baat'ili, na bishara na onyo, na kuzitengeneza nafsi, na kupiga mifano, na kubainisha hukumu. Nacho kinasomwa kwa ulimi wa Kiarabu, chepesi kukifahamu kwa watu wanao jua.

4 Chenye kuwapa khabari njema Waumini wenye kutenda kuwa watapata neema iliyo andaliwa kwa ajili yao, na kuwakhofisha wanao kanusha kuwa watapata adhabu chungu iliyo andaliwa kwa ajili yao. Lakini wengi walikutipilia mbali, wala wasinafiike nacho, kama kwamba hawakusikia.

5 Na makafiri wakamwambia Mtume s.a.w.: Nyoyo zetu zimo katika vifuniko vizito kwa hayo unayo tuitia yaliyo khusu Tawhidi (Upweke) wa Mwenyezi Mungu. Na masikioni mwetu mna uziwi, basi hayasikii hayo unayo tulingania. Na baina yetu na wewe lipo pazia nene linalo tuzuia kukubali hayo uliyo tuletea. Basi fanya utakalo, na sisi tunafanya tutakalo.

6 Ewe Mtume! Waambie: Hakika mimi si chochote ila ni mtu mfano wenu nyinyi, napata Wahyi (Ufunuo) kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwamba wa kuabudiwa kwa haki na nyinyi ni Mungu Mmoja tu. Basi fuateni Njia Iliyo Nyooka ya kwendea kwake! Na mtake kwake msamaha kwa madhambi yenu. Na washirikina wasio toa Zaka kuwapa wanao stahiki watapata adhabu kali. Na wao tu, si wenginewe, ndio wanao kataa kuwa upo uhai wa Akhera.

7 Tazama tanbihi ya 6.

8 Hakika Waumini wanao tenda mema watapata malipo mazuri yasiyo katika.

9 Ewe Mtume! Waambie hawa washirikina: Ama nyinyi mnastaajabisha! Mnamkataa Mwenyezi Mungu aliye iumba ardhi kwa siku mbili, na huku juu ya hayo, mnamfanyia washirika wa kushirikiana naye huyo Muumba ardhi, Mmiliki wa walimwengu wote na Mlezi wao? (*Tazama Maelezo 41:9*)

10 Naye Mwenyezi Mungu amesimamisha juu ya ardhi milima iliyo simama imara ili isiyumbe nanyi; na akakithirisha humo kheri nyingi, na akakadiria humo riziki kwa watu wake, kwa mujibu wa hikima yake, mnamo siku nne. Na nyinyi, juu ya haya, mnakwenda kumwekea washirika? Na Yeye amekadiria kila kitu bila ya upungufu wala kuzidi. Kufafanua huku katika uumbaji wa ardhi na vilio juu yake ni maelezo

- 11.** Kisha akazielekea mbingu, na zilikuwa moshi, akaziambia hizo na ardhi: Njooi, kwa khiari au kwa nguvu! Vyote viwili vikasema: Tumekuja nasi ni wat'iifu.¹¹
- 12.** Basi akazifanya mbingu saba kwa siku mbili, na akazipangia kila mbingu mambo yake. Na tukaipamba mbingu ya chini kwa mataa na kwa ulinzi. Hichi ndicho kipimo cha Mwenyezi Mungu Mwenye Kujua.¹²
- 13.** Basi wakipuuzwa wewe sema: Nakuhadharisheni adhabu mfano wa adhabu ya A'di na Thamudi,¹³
- 14.** Walipo wajia Mitume mbele yao na nyuma yao wakawaambia: Msimuabudu ila Mwenyezi Mungu! Wakasema: Angeli taka Mola wetu Mlezi bila ya shaka angeli wateremsha Malaika. Basi sisi hakika tunayakataa hayo mliyo tumwa.¹⁴
- 15.** Ama kina A'di walijivuna katika nchi bila ya haki, na wakasema: Nani aliye kuwa na nguvu kushinda sisi? Kwani wao hawakuona kwamba Mwenyezi Mungu aliye waumba ni Mwenye nguvu kushinda wao? Na wao wakawa wanazikataa Ishara zetu!¹⁵
- 16.** Basi tuliwapelekea upepo wa kimbunga katika siku za ukorofi, ili tuwaonjeshe adhabu ya kuwahizi katika uhai wa duniani, na bila ya shaka adhabu ya Akhera ina hizaya zaidi, na wala wao hawatanusuriwa.¹⁶
- 17.** Na ama Thamudi tuliwaongoza, lakini walipenda upofu kuliko uwongofu. Basi uliwachukua moto wa adhabu ya kuwafedhehi kwa sababu ya yale waliyo kuwa wakiyachuma.¹⁷
- 18.** Na tukawaokoa walio amini na wakawa wanamcha-mngu.¹⁸
- 19.** Na siku watakapo kusanywa maadui wa Mwenyezi Mungu kwenye Moto, nao wakigawanywa kwa makundi.¹⁹

kwa hao wanao uliza.

11 Kisha amekhusisha uweza wake na kuumba mbingu, nazo zilikuwa kama moshi, basi zikawapo. Na kuumba kwake mbingu na ardhi kwa mujibu wa mapendo yake ni jambo jepesi kwake, ni kama kukiambia kitu: Njoo ukipenda usipenda, nacho kikat'ii.

12 Na akatimiza kuumba mbingu saba mnamo siku mbili nyengine. Na akaweka katika kila mbingu alichokandalia na ilivyo pelekea hikima yake. Na akaipamba mbingu ya karibu na dunia kwa nyota zinazo ng'ara kama taa, kwa ajili ya uwongofu wasisikilize mashetani khabari za walio juu. Kuumba huko vilivyo ni mpango wa Mwenyezi Mungu asiye shindika, Mwenye kuzunguka kila kitu.

13 Basi washirikina wakipuuzwa Imani baada ya kuwekewa wazi dalili zake, wewe, Mtume, waambie: Nimekuonyeni msije kupatilizwa kwa adhabu kali kama iliyo wateketeza kina A'di na Thamudi.

14 Walijiwa A'di na Thamudi na hiyo adhabu walipo watokelea Mitume pande zote. Hawakuacha njia ya kuwaongoza ila waliipitia, na wakawaambia: Msimuabudu ila Mwenyezi Mungu. Wao wakasema: Lau Mwenyezi Mungu angeli taka kumtuma Mtume basi angeli tuteremshia Malaika. Basi sisi hakika tunakataa hayo ya Tawhidi na mengineyo mliyo kuja nayo nyinyi.

15 Ama kina A'di walipandwa na kiburi katika nchi bila ya haki ya kuwa na kiburi hicho. Na walisema kwa kughurika na nafsi zao: Nani huyo anaye tushinda sisi kwa nguvu? Ama ajabu watu hawa! Wanasema hayo na wao hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu aliye waumba ana nguvu zaidi kuwashinda wao? Na wao walikuwa wakizikanya Ishara zetu!

16 Tukawapelekea upepo wenye sauti kali katika siku korofi, ili tuwaonjeshe adhabu ya kuwafanya wawe madhalili wanyonge katika maisha ya duniani. Na ninaapa kuwa bila ya shaka adhabu ya Akhera itakuwa ya hizaya zaidi, wala wao siku hiyo hawatapata wa kuwasaidia.

17 Na ama kina Thamudi tuliwabainishia njia ya kheri na njia ya shari. Lakini wao walikhiari upotovu kuliko uwongofu, ikawatwaa radi iliyo waunguza kwa madhila na unyonge, kwa sababu ya madhambi waliyo yachuma.

18 Na tukawaokoa kutokana na adhabu hii wale walio amini, na wakawa wanamcha Mwenyezi Mungu na wanaigopa adhabu yake.

19 Ewe Nabii! Siku watakapo kusanywa maadui wa Mwenyezi Mungu kupeleka Motoni, wakawa wa

- 20.** Hata watakapo ufikia Moto yatawashuhudia masikio yao, na macho yao na ngozi zao kwa waliyo kuwa wakiyatenda.²⁰
- 21.** Na wao wataziambia ngozi zao: Kwa nini mmetushuhudilia? Nazo zitasema: Ametutamkisha Mwenyezi Mungu ambaye ametamkisha kila kitu! Na Yeye ndiye aliye kuumbeni mara ya kwanza, na kwake Yeye tu mtarejeshwa.²¹
- 22.** Na hamkuwa wenye kujificha hata masikio yenu, na macho yenu, na ngozi zenu, zisikushuhudilieni. Lakini mlidhani kwamba Mwenyezi Mungu hayajui mengi katika mliyo kuwa mkiyatenda.²²
- 23.** Basi hiyo dhana yenu mliyo kuwa mkimdhania Mola wenu Mlezi. Imekuamamizeni; na mmekuwa miongoni mwa walio khasiri.²³
- 24.** Basi wakisubiri Moto ndio maskani yao. Na wakiomba radhi hawakubaliwi.²⁴
- 25.** Na tukawawekea marafiki, na wakawapambia yaliyo mbele yao na nyuma yao. Basi ikawathibitikia kauli wawe pamoja na mataifa yaliyo pita kabla yao, miongoni mwa majini na watu. Hakika hao wamekuwa ni wenye kukhasirika.²⁵
- 26.** Na walio kufuru walisema: Msiisikilize Qur'ani hii, na timueni zogo, huenda mkashinda.²⁶
- 27.** Basi hapana shaka tutawaonjesha hao walio kufuru adhabu kali, na hapana shaka tutawalipa malipo mabaya ya yale waliyo kuwa wakiyafanya.²⁷
- 28.** Hayo ndiyo malipo ya Maadui wa Mwenyezi Mungu - Moto! Humo watakuwa na maskani ya kudumu, ndiyo malipo yao kwa sababu walikuwa wakizikataa Ishara zetu.²⁸
- 29.** Na walio kufuru watasema: Mola wetu Mlezi! Tuonyeshe walio tupoteza miongoni

mwanzo wao wanakutana na wa mwisho wao, ili ipate hoja ilazimike juu ya wote.

20 Mpaka watakapo ufikia Moto na wakaulizwa juu ya madhambi waliyo yatenda duniani, na wao wakakataa, yakawashuhudilia masikio yao, na macho yao, na ngozi zao kwa waliyo yatenda wao.

21 Na hao maadui wa Mwenyezi Mungu wakaziambia ngozi zao: Kwa nini mmetushuhudilia? Na ngozi zitasema: Ametutamkisha Mwenyezi Mungu aliye tamkisha kila kitu. Na Yeye ndiye aliye kuumbeni hapo mwanzo kabla hamjawa chochote. Na kwake Yeye, peke yake, ndio mtarejea baada ya kufufuliwa, akuhisabieni mliyo kwisha yatanguliza katika vitendo.

22 Wala nyinyi hamkuwa mkiweza kuficha vitendo vyenu viovu hata viungo vyenu visivione na ikawa macho yenu, na masikio yenu na ngozi zenu, vyote hivyo vikakushuhudilieni. Lakini nyinyi mlikuwa mkidhani kuwa Mwenyezi Mungu hajui mengi katika vitendo vyenu, kwa sababu mkivifanya kwa uficho.

23 Lakini dhana mbovu mliyo kuwa mkimdhania Mola wenu Mlezi imekuhilikini, na kwa hivyo mmekuwa Siku ya Kiyama katika wenye kukhasiri vibaya mno.

24 Basi hata wakijizua machungu yao, Moto ndio mwisho wao, na makaazi yao ya daima. Na wakitaka kumridhi Mwenyezi Mungu sasa hawakubaliwi hayo matakwa yao.

25 Nasi tumewaandalia duniani marafiki waharibifu, na wao wakawazainishia mbele yao mambo ya Akhera, basi wakawaghuri kwamba ati hakuna kufufuliwa wala kuhisabiwa, na wakawapambia pia mambo ya duniani ili wastarehe nayo. Na neno la adhabu lilio wapata mataifa yaliyo kwisha pita miongoni mwa majini na watu walio kuwa kama wao, likawathibitikia na wao kwa sababu ya kukhiari kwao upotovu badala ya uwongo. Hakika watu hao wote walikuwa katika walio khasiri khasara iliyo timia.

26 Makafiri wakaambizana wenyewe kwa wenyewe: Msiisikilize hii Qur'ani, na inapo somwa nyie leteni porojo lisio kuwa na maana, ili pasiwepo mtu wa kuisikia wala kunafika kwayo, asaa kwa hivyo mkamshinda Muhammad.

27 Tunaapa: Bila ya shaka tutawaonjesha walio kufuru adhabu kali kwa vitendo vyao, na khasa kwa hivi kuipiga vita Qur'ani. Na bila ya shaka tutawalipa malipo maovu kabisa kwa vitendo vyao.

28 Hizo adhabu zilizo tajwa ni malipo wanayo stahiki maadui wa Mwenyezi Mungu - Moto walio andaliwa katika makaazi ya kuishi milele, kuwa ni malipo kwa kule kuzikataa mfululizo Ishara za Mwenyezi Mungu na hoja zake.

mwa majini na watu ili tuwaweke chini ya miguu yetu, wapate kuwa miongoni wa walio chini kabisa.²⁹

30. Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msio gope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyo kuwa mkiahidiwa.³⁰

31. Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata kinacho tamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyo vitaka.³¹

32. Ni takrima itokayo kwa Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.³²

33. Na ni nani mborwa wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu?³³

34. Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu.³⁴

35. Lakini hawapewi wema huu ila wanao subiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa.³⁵

36. Na Shet'ani akikuchochea kwa uchochezi wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.³⁶

37. Na katika Ishara zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi. Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu aliye viumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu.³⁷

38. Na ikiwa watajivuna, basi hao walioko kwa Mola wako Mlezi wanamtakasa Yeye usiku na mchana, na wao hawachoki.³⁸

29 Na makafiri watasema, nao wamo Motoni: Mola wetu Mlezi! Tuonyeshe hayo makundi ya majini na watu walio tupoteza ili tuwaweke chini ya nyayo zetu, wawe katika watu wa chini kabisa.

30 Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu, kwa kuukubali Upweke wake, kisha wakasimama sawa sawa juu ya sharia zake, Malaika watawateremkia mara kwa mara wakiwaambia: Msikhofu kukuteremkieni shari, wala msihuzunike kuwa mtakosa kheri, na furahini kuwa mtapata Pepo mliyo ahidiwa kwa ndimi za Manabii na Mitume.

31 Na Malaika watawaambia: Sisi ni wasaidizi wenu katika maisha ya duniani kwa kukuunjeni mkono, na Akhera kwa kukuombeeni shafaa na kukutukuzeni. Na huko Akhera mtapata kila cha ladha na kizuri kinacho pendwa na nafsi zenu, na mtapata kila mnacho kitamani kuwa ni takrima, na maamkio yanayo toka kwa Mola Mlezi Mkunjufu wa maghfira na rehema.

32 Tazama tanbihi ya 31.

33 Hapana mwenye kauli nzuri zaidi kuliko mwenye kulingania Tawhid ya Mwenyezi Mungu na ut'iifu wake, na pamoja na hayo, akatenda vitendo vyema, na akasema kwa kuungama itikadi yake: Hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu, yaani wenye kunyenyekea amri za Mwenyezi Mungu.

34 Haziwezi kuwa sawa tabia njema na tabia mbovu. Pinga uovu ukikujia kutokana na adui kwa tabia iliyo bora kuliko yake. Hapo matokeo yake ni huyo ambaye uliye kuwa na uadui naye atakuja kuwa kama mwenzio wa kukunusuru mwenye moyo safi.

35 Na hawaruzukiwi tabia hii, ya kulipa wema kwa uovu, ila wale wenye khulka ya kusubiri, na hawaruzukiwi hayo ila wenye fungu kubwa la tabia ya wema na ukamilifu wa nafsi.

36 Na akitokea Shetani akakutia wasiwasi kukuachisha hayo uliyo amrishwa, ewe unaye semezwa, basi jilinde naye kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu kusikia kwake na kujua kwake kumezunguka kila kitu. Na Yeye atakulinda naye.

37 Na katika dalili za uweza wake Mwenyezi Mungu Mtukufu ni huu usiku na mchana, na jua na mwezi. Msilisujudie jua wala mwezi, kwani hivyo ni katika Ishara zake tu. Bali msujudieni Yeye Mwenyezi Mungu peke yake, aliye umba jua, na mwezi, na usiku, na mchana, ikiwa nyinyi kweli mnamuabudu Yeye peke yake.

38 Ikiwa washirikina watajiona wakubwa hawafai kufuata amri yako, basi wewe usiudhike. Kwani hao walio kwa Mola wako Mlezi kwenye utakatifu wake, nao ni Malaika, wanamtakasa Yeye na kila

- 39.** Na katika Ishara zake ni kwamba unaiona ardhi nyonge, lakini tunapo iteremshia maji mara unaiona inataharaki na kuumuka. Bila ya shaka aliye ihuisha ardhi ndiye atakaye huisha wafu. Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.³⁹
- 40.** Hakika wale wanao upotoa ukweli uliomo katika Ishara zetu hawatufichikii Sisi. Je! Atakaye tupwa Motoni ni bora au atakaye kuja kwa amani Siku ya Kiyama? Tendeni mpendavyo, kwa hakika Yeye anayaona mnayo yatenda.⁴⁰
- 41.** Kwa hakika wanayo yakataa mawaidha haya yanapo wajia (wataangamia), na haya bila ya shaka ni Kitabu chenye nguvu na utukufu.⁴¹
- 42.** Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye hikima, Msifiwa.⁴²
- 43.** Huambiwi ila yale yale waliyo ambiwa Mitume wa kabla yako. Hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka ni Mwenye maghfira, na ni Mwenye adhabu chungu.⁴³
- 44.** Na lau tungeli ifanya Qur'ani kwa lugha ya kigeni wangu semu: Kwanini Aya zake haziku pambanuliwa? Yawaje lugha ya kigeni na Mtume Mwaarabu? Semu: Hii Qur'ani ni uwongofu na poza kwa wenye kuamini. Na wasio amini umo uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni. Hao wanaitwa nao wako pahala mbali.⁴⁴
- 45.** Na hakika tulimpa Musa Kitabu, lakini pakatokea khitilafu kati yake. Na lau kuwa halikwisha tangulia neno la Mola wako Mlezi wangu hukumiwa. Na hakika wao wamo katika shaka yenye kuwatia wasiwasi.⁴⁵

upungufu katika kila wakati, usiku na mchana, wakimsafia ibada Yeye tu, wala hawachoki kumsabihi.

39 Na katika dalili za uweza wake, Mtukufu, ni kwamba unaona, wewe unaye weza kuona, ardhi kavu. Tukiiteremshia maji inatikusika kwa mimea, na inaumuka na kuja juu. Hakika huyo aliye ihuisha ardhi iliyo kwisha kufa ndiye aliye elekea kuhuisha wafu katika hayawani. Yeye ni mtimilivu wa uweza juu ya kila kitu. (*Tazama Maelezo 41:39*)

40 Hakika hao wanao iacha Njia iliyo sawa kwa mintarafu ya Ishara zetu na wakaitupilia mbali kwa kuikadhibisha, mambo yao hayatupotei Sisi wala hayo wanayo yakusudia. Nasi tutawalipa kama wanavyo stahiki. Kwani anaye tupwa katika Moto ni bora au yule anaye kuja naye hali katulia Siku ya Kiyama kwa kuokoka kwake na kila ovu? Kabisa hao hawalingani. Waambie kwa kuwaahidi: Fanyeni mtakavyo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuzunguka kila kitu kwa jicho lake, naye atamlipa kila mmoja kwa a'mali yake.

41 Hakika wanao ikataa Qur'ani Tukufu inapo wajia bila ya kuzingatia, watapata adhabu ambayo hapana mtu anaye weza kuikadiria. Wao wameipinga Qur'ani nacho hakika ni Kitabu kisicho kuwa na mfano, kinamshinda kila mwenye kukipinga, hakiingiliwi na upotofu usio kuwa na asli kwake kwa upande wowote ule, kimeteremka kwa kukufuatana kutokana na Mungu aliye takasika na upuuzi, Msifiwa kwa wingi wa sifa kwa neema alizo zitoa.

42 Tazama tanbihi ya 41.

43 Ewe Muhammad! Huambiwi wewe na maadui wako ila kama walivyo ambiwa Mitume wa kabla yako na maadui wao, nayo ni matusi na kuambiwa mwongo. Hakika Muumba wako na Mlezi wako ana msamaha mwingi, na ni Mwenye kuadhibu kwa machungu makubwa. Basi Yeye humghufiria mwenye kutubu kwake, na humtesa mwenye kushikilia na inda yake.

44 Na lau tungeli ifanya Qur'ani kwa lugha ya kigeni, kama walivyo pendekeza baadhi ya hao wanao kera, basi bila ya shaka wangu semu: Lau zingeli bainishwa Aya zake kwa ulimi tunao ufahamu! Kitabu hichi cha lugha ya kigeni, na huyu mkhubiri wake ni Mwaarabu! Yawaje haya? Ewe Mtume! Waambie: Hii Qur'ani ni hivyo hivyo kama walivyo teremshiwa Waumini, si wengineo, kuwa ni Uwongofu na Poza kwa Waumini; kiwaokoe na ubabaishi, na kiwaponyeshe na shaka shaka. Na wasio amini wamekuwa kama katika masikio yao pana kizuizi, uziwi, nayo hii Qur'ani kwao wao ni upofu, hawaoni chochote ndani yake ila fitna tu. Hao makafiri ni kama wanao itwa waiamini kwa umbali kabisa. Hawausikii wito huo.

45 Ninaapa: Kwa hakika tulimpa Musa Taurati, na watu wake wakakhitalifiana kwayo. Na lau ingeli kuwa hukumu ya Mola wako Mlezi haikuakhirishwa, ewe Muhammad, mpaka muda maalumu kwake,

46. Anaye tenda mema basi anajitendea mwenyewe nafsi yake, na mwenye kutenda uovu basi ni juu ya nafsi yake vile vile; wala Mola wako Mlezi si mwenye kuwadhulumu waja.⁴⁶

47. UJUZI wa kuijua Saa ya Kiyama unarudishwa kwake tu Mwenyezi Mungu. Na matunda hayatoki katika mafumba yake, wala mwanamke hachukui mimba, wala hazai, ila kwa kujua kwake. Na siku atakayo waita, akawaambia: Wako wapi washirika wangu? Hapo watasema: Tunakiri kwako ya kwamba hapana miongoni mwetu anaye shuhudia hayo.⁴⁷

48. Na wakawapotea wale walio kuwa wakiwaomba hapo kwanza, na wakawa na yakini kuwa hawana pa kukimbilia.⁴⁸

49. Mwanaadamu hachoki kuomba dua za kheri, na inapo mpata shari, mara huvunjika moyo akakata tamaa.⁴⁹

50. Na pindi tukimwonjesha rehema itokayo kwetu baada ya kumgusa dhara, bila ya shaka husema: Haya nayastahiki mimi, wala sidhani kuwa Kiyama kitakuja. Na hata nikirudishwa kwa Mola wangu Mlezi bila ya shaka nina mema yangu kwake! Basi kwa yakini tutawaelezea walio kufuru hayo waliyo yatenda, na kwa yakini tutawaonjesha adhabu ngumu.⁵⁰

51. Na tukimneemesha mwanaadamu hugeuka na kujitenga upande, na inapo mgusa shari, huwa na madua marefu marefu.⁵¹

52. Sema: Mnaonaje! Ikiwa haya yanatoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi ikawa ndio mmeyakataa, ni nani aliye potea zaidi kuliko aliye katika upinzani wa mbali?⁵²

53. Tutawaonyesha Ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba Mola wako Mlezi

basi hapana shaka pange amuliwa hukumu baina yako na hao kwa kuwang'olea mbali wanao kanusha. Na hakika makafiri katika kaumu yako wamo katika shaka na Qur'ani, na hiyo inawatia dhiki na wasiwasi.

46 Mwenye kutenda vitendo vyema ujira wake ataupata mwenyewe, na mwenye kutenda uovu madhambi yake yatakuwa juu yake. Na Mola wako Mlezi si mwenye kuwadhulumu waja wake, hata amtese mtu kwa dhambi za mwengine.

47 Kwa Mwenyezi Mungu peke yake ndio unarejea ujuzi wa kusimama Saa ya Kiyama. Matunda hayatoki kwenye vifuniko vyake, wala mwanamke hachukui mimba wala hazai ila awe Yeye anajua. Na kumbuka siku ambayo Mwenyezi Mungu atawaita washirikina, kwa kuwakebehi, awaambie: Wako wapi hao washirika wangu mlio kuwa mkiwaomba badala yangu? Watasema kwa kutaadhari: Ewe Mwenyezi Mungu! Tunakujavya kuwa sisi hatuna wa kushuhudia kuwa wewe una mshirika yeyote.

48 Na hao miungu ya ushirikina walio kuwa wakiwaabudu watawapotea, na waliyakinika kuwa hawana pa kukimbilia.

49 Mwanaadamu hachoki kumwomba Mola wake Mlezi kwa kheri za kidunia. Ikimpata shari basi huwa mwingi wa kuikatia tamaa kheri, na kuvunjika moyo hadi, ya kwamba Mwenyezi Mungu hamwitikii dua yake.

50 Tunaapa: Tukimwonjesha mtu neema, kwa fadhila yetu, baada ya dhara kubwa iliyo msibu bila ya shaka husema: Hii neema niliyo ipata ni haki yangu mimi. Wala sidhani kuwa Kiyama kitakuja. Na ninaapa ikitokea nikarejeshwa kwa Mola wangu Mlezi basi na huko kwake bila ya shaka nitapata malipo mema. Lakini Sisi tunaapa: Hapana shaka tutawalipa walio kufuru, Siku ya Kiyama, kwa vitendo vyao! Na hapana shaka tutawaonjesha adhabu kali iliyo rindikwa juu kwa juu.

51 Na tukimneemesha mtu huacha kutushukuru, na akajitenga mbali na Dini yetu. Na tukimwonjesha shari basi huwa mwingi wa kuomba madua.

52 Ewe Muhammad! Waambie: Hebu nambieni; ikiwa hii Qur'ani imetoka kwa Mwenyezi Mungu nanyi mkawa mnaikataa, basi nani aliye kuwa mbali mno na Ukweli kuliko huyo aliye kinyume na Haki?

kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?⁵³

54. Ama wao wamo katika shaka ya kukutana na Mola wao Mlezi! Ama hakika Yeye amekizunguka kila kitu.⁵⁴

53 Karibuni hivi tutawaonyesha hao wanao zikataa Ishara zetu zenye kuonyesha ukweli wako katika pande za mbinguni na ardhi, na katika nafsi zao wenyewe, mpaka yawadhihirikie ya kwamba uliyo waletea ni Haki tupu si vinginevyo. Je! Wanakataa kuwa Sisi tunawaletea Ishara hizo? Je! Haitoshi kuwa Mola wako Mlezi ni Mwenye kukizunguka kila kitu.

54 Ama hakika hawa makafiri wamo katika shaka kubwa kukutana na Mola wao Mlezi, kwa sababu ya kuwa hawaamini kufufuliwa. Ama hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukizunguka kila kitu kwa ujuzi wake na uweza wake.

Sura 42 - Ash-Shuura

Utangulizi

Hii ni Sura ya Makka, na idadi ya Aya zake ni 53, na imeitwa *Ash-shuura*, yaani “Kushauriana” kwa sababu inavyo waongoza Waumini waendeshe mambo ya jamii zao kwa kushauriana, ili ipatikane Haki, na uthibiti uadilifu. Na Sura hii imekusanya mambo mengi ya Dini na hoja za itikadi.

Imefungua Sura kwa kuisifu Qur’ani yenyewe kwa kuwa ni Wahyi (Ufunuo) ulio toka kwa Mwenyezi Mungu, ikayarudisha matusi ya makafiri, na ikashughulikia kumpoza Mtume s.a.w., na tena baada ya hayo ikaingilia kuthibitisha uweza wa Mwenyezi Mungu aliye iteremsha Qur’ani na ukatukuka utawala wake, na ikaeleza kukanya kwa baadhi ya watu juu ya kuwa hoja zake ziwazi zinazo onyesha kuwa haya yanatoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa kubainisha khitilafu zao katika kufahamu Haki. Na baada yake Sura hii ikatilia mkazo uweza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya kila kitu. Kisha ikathibitisha kuwa msingi wa sharia ni mmoja, na ikaashiria kuwa wapo wanao kufuru juu ya hivyo. Hali kadhaalika imeashiria kuwa Vitabu vyote vya mbinguni vinaongoza kwenda Haki. Na Sura imelaani shirki ya washirikina, na kukhitalifiana kwao katika Haki kwa udhalimu tu. Na pia imelaani kule kuhimiza kwao, wanao kadhibisha, kuhimiza Kiyama kwa maskhara. Na ikatoa uwongozi kwa wafuasi wake wawalinganie watu kwenye Dini, kama ilivyo eleza ubora wa upole wa Mwenyezi Mungu kwa waja wake. Na Sura hii imehadharisha kuzama katika kuiwania dunia tu peke yake. Na ikabainisha uovu wa hali ya makafiri na wema wa hali ya Waumini katika Akhera. Na Sura ikawalaumu wale walio mkadhibisha Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. kwa kumwambia kaizua Qur’ani, hali wao wameshindwa hata kuleta Sura moja tu mfano wake. Kisha ikatangaza kuwa Mwenyezi Mungu ameikubali toba ya Waumini, na ikatangaza hikima ya kuzigawa riziki kwa watu kwa mpango wa hikima. Hawakuwa wote matajiri, kwa kuchelea wasipande jeuri, wala wasiwe wote mafakiri wakateketea. Bali amewakunjulia baadhi na amewadhikisha wengine.

Na akadhihirisha baraka za mvua, na dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu kwa jambo hili, na kwamba masaibu ya dunia ni kwa sababu ya maasi. Kisha *Subhanahu* akakariri kwa njia nyingine hali za Waumini na wanao kadhibisha huko Akhera, na madhila yatayo wapata wanao kadhibisha. Na akataka wafanye haraka kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu kabla uhai haujakata fursa ya kutenda. Kadhaalika Sura imeshughulika kumpoza Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. na kubainisha uweza wake *Subhanahu* kumtunukia amtakaye watoto wa kike, na wa kiume mwenginewe, na mchanganyiko kwa wa tatu, na kumnyima kabisa wa nne. Kisha Sura ikataja njia za Mwenyezi Mungu kusema na Manabii wake, na ikakhitimisha kwa kubainisha Njia ya Haki Iliyo Nyooka ambayo inayo pasa kuifua

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. H'a Mim¹

2. A'yn Sin Qaf²

3. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu na Mwenye hikima anavyo kuletea Wahyi wewe na walio kabla yako.³

4. Ni vyake viliomo mbinguni, na viliomo katika ardhi. Na Yeye ndiye Mtukufu, Mkuu.⁴

5. Zinakaribia mbingu kupasuka juu huko, na Malaika wakimtakasa Mola wao Mlezi na kumhimidi, na wakiwaombea maghfira waliomo kwenye ardhi. Ama hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁵

6. Na wale walio wafanya walinzi wengine badala yake Yeye, Mwenyezi Mungu ni Mwangalizi juu yao. Wala wewe si wakili juu yao.⁶

7. Na namna hivi tumekufunulia Qur'ani kwa Kiarabu ili uwaonye watu wa Mama wa Miji na walio pembezoni mwake. Na uhadharishe na Siku ya Mkutano, haina shaka hiyo. Kundi moja litakuwa Peponi, na kundi jengine Motoni.⁷

8. Na Mwenyezi Mungu angeli penda ange wafanya wote umma mmoja, lakini anamwingiza katika rehema yake amtakaye. Na wenye kudhulumu hawana mlinzi wala msaidizi.⁸

9. Au wamechukua walinzi wengine badala yake! Lakini Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi khasa. Na Yeye ndiye anaye huisha wafu. Na Yeye ndiye Mweza wa kila kitu.⁹

1 H'a Mim, A'yn Sin Qaf: Sura imeanzia kwa harufi hizi za kutamkwa kama ilivyo ada katika Sura nyingi katika Qur'ani.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Mfano wa yaliyomo katika Sura hii anakufunulia wewe na Mitume walio kuwa kabla yako, Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda kwa nguvu zake, ambaye amepanga kila kitu kwa pahala pake, kwa mujibu wa hikima katika vitendo vyake na mipango yake.

4 Ni vya Mwenyezi Mungu, peke yake, vyote viliomo katika mbingu na ardhi, kwa kuviumba, kuvimilika, na kuviendesha. Naye ni peke yake aliyetukuka kwa nafsi, na ukawa mkuu ufalme wake.

5 Mbingu, juu ya ukubwa wake na kushikamana kwake, zimekaribia kupasuka kutoka huko juu kwa kumwogopa Mwenyezi Mungu, na kuathirika kwa taadhima yake na utukufu wake. Na Malaika wanamtakasa Mwenyezi Mungu na kila lisilo elekea naye, na humsifu kwa analo stahiki. Na humwomba Mwenyezi Mungu awasamehe watu wa duniani. Na Yeye *Subhanahu* ananabihisha kwamba hakika ni Mwenyezi Mungu tu, peke yake, ndiye Mwenye maghfira ya wote, na rehema iliyo kunjufu.

6 Na hao walio wafanya wengineo badala ya Mwenyezi Mungu kuwa ndio wa kuwanusuru, Mwenyezi Mungu anaangalia hayo wayatendayo. Wala wewe hukupewa kazi hiyo ya kuwaangalia wao.

7 Na mfano wa ufunuo huo ulio wazi, tumekufunulia wewe hii Qur'ani kwa lugha ya Kiarabu isiyo na ubabaishi, ili upate kuwaonya watu wa Makka na walio pembezoni mwake katika Waarabu, na uwaonye watu adhabu ya siku watakao kusanywa khalaiiki wote kwa ajili ya hisabu. Hapana shaka yoyote kuja siku hiyo. Watu siku hiyo watakuwa mafungu mawili - fungu moja litakuwa Peponi. ma kundi jengine litakuwa Motoni.

8 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli penda kuwakusanya watu wote katika dunia wakafuata njia moja angeli wakusanya hivyo. Lakini Yeye humtia katika rehema yake amtakaye, kwa kuwa anajua kuwa hao wamekhiari uwongofu kuliko upotofu. Na wenye kujidhulumu nafsi zao kwa ukafiri hawana mlinzi badala ya Mwenyezi Mungu wa kudhamini kuwalinda, wala msaidizi wa kuwaokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

9 Hawa wenye kudhulumu hawakumfanya Mwenyezi Mungu kuwa ni mlinzi wao, bali wamewafanya wengineo kuwa ndio walinzi wao. Na wala haiwafalii wao hayo. Kwani Mwenyezi Mungu, peke yake,

10. Na mkikhitalifiana katika jambo lolote, basi hukumu yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Huyu Mwenyezi Mungu ndiye Mola wangu Mlezi, ninaye mtegemea na kwake Yeye narejea.¹⁰

11. Yeye ndiye Muumba mbingu na ardhi, amekujaalieni mke na mume katika nafsi zenu, na katika nyama hoa dume na jike, anakuzidishieni namna hii. Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.¹¹

12. Yeye ndiye Mwenye funguo za mbingu na ardhi. Humkunjulia riziki amtakaye, na humpimia amtakaye. Hakika Yeye ni Mjuzi wa kila kitu.¹²

13. Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo. Ni magumu kwa washirikina hayo unayo waitia. Mwenyezi Mungu humteua kwake amtakaye, na humwongoa kwake aelekeaye.¹³

14. Na hawakufarikiana ila baada ya kuwajia ilimu kwa sababu ya husuda iliyo kuwa baina yao. Na lau kuwa haikwisha tangulia kauli kutoka kwa Mola wako Mlezi ya kuakhirisha mpaka muda maalumu, basi bila ya shaka palingeli hukumiwa baina yao. Na hakika walio rithishwa Kitabu baada yao wanakitilia shaka inayo wahangaisha.¹⁴

15. Basi kwa haya waite! Nawe simama sawa sawa kama ulivyo amrishwa, wala usiyafuate matamano yao. Na sema: Naamini aliyo teremsha Mwenyezi Mungu katika Vitabu. Na nimeamrishwa nifanye uadilifu baina yenu. Mwenyezi Mungu ni Mola wetu Mlezi, na Mola wenu Mlezi. Sisi tuna jukumu kwa vitendo vyetu, na nyinyi mna

ndiye Mwenye kustahiki kuwa Mlinzi kama wao wanataka mlinzi. Yeye ndiye anaye fufua walio kufa kwa ajili ya hisabu. Na Yeye ndiye Mwenye madaraka juu ya kila kitu kwa uweza wake.

10 Na mliyo khitalifiana kwayo katika mambo yaliyo khusu Imani na ukafiri, hukumu yake ya kukata iko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye amekwisha ibainisha. Yeye huyo ndiye Hakimu wa kuhukumu mliyo khitalifiana, Mwenyezi Mungu, Mwenye kumiliki mambo yangu yote. Mimi namtegemea Yeye kwa mambo yangu. Na kwake Yeye peke yake ndio narejea ili kutafuta uwongozi.

11 Yeye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi, na akakuumbieni katika jinsi yenu wanaume na wanawake, na akaumba katika mifugo yenu kadhaalika madume na majike, na kwa mpango huu ndio wazidi kuwa wengi. Hapana kitu chochote kama mfano wake Mwenyezi Mungu, basi hana kitu cha kuwa wa pili yake. Na Yeye ndiye Mwenye kujua, kwa ujuzi wa kukamilika, kuvijua vyote vinavyo sikilizana na kuonekana bila ya taathira ya hisiya.

12 Yeye Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye funguo za mbingu na ardhi, kwa kuzihifadhi na kuzitumia. Humkunjulia riziki amtakaye, na humdhikisha amtakaye. Hakika Yeye, Mtukufu, ujuzi wake umezunguka kila kitu.

13 Amekufanyieni sharia itikadi kama alivyo agana na Nuhu, na tulizo kufunulia wewe kwa Wahyi, na tulivyo agana na Ibrahim, na Musa, na Isa, ya kwamba mazitie imara nguzo za Dini, kwa kuyafuata yaliyo letwa na Dini, wala msikhitalifiane katika jambo hilo. Ni uzito kwa washirikina hayo unayo waitia ya kusimamisha nguzo za Dini. Mwenyezi Mungu humteuwa kwa ajili ya Ujumbe wake amtakaye, na humwezesha na kumsaidia katika Imani na kusimama katika Dini mwenye kuacha inda na kumwelekea Yeye

14 Wala hawakukhitalifiana katika Dini wafuasi wa Mitume walio tangulia ila baada ya kuwafikia ujuzi wa kweli, na hayo ni kwa kutokana na uadui na uhasidi ulio baina yao. Na lau kuwa si ahadi iliyo kwisha tangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu ya kuakhirisha adhabu mpaka Siku ya Kiyama, basi bila ya shaka walingeli teketezwa. Na kwa hakika wale walio rithishwa Kitabu kutokana na walio kabla yao, na wakawahi zama zako, wana shaka na Kitabu chao, tena shaka ya kuwatatanisha. Ndio maana hawaitikii wito wako. (Lau kuwa Mayahudi wameamini kweli yaliyomo katika Taurati, wangu muamini Nabii Isa na Nabii Muhammad. Na lau kuwa Wakristo wameamini kweli yaliyomo katika Taurati na Injili basi hapana la kuwazuia wasimuamini Nabii Muhammad, na kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja, wala hana Utatu. Lakini hawana imani ya yakini, na kwa hivyo wameunda mawazo yaliyo nje ya Taurati na nje ya Injili.)

jukumu kwa vitendo vyenu. Hapana kuhojiana baina yetu na nyinyi. Na Mwenyezi Mungu atatukusanya pamoja, na marejeo ni kwake.¹⁵

16. Na wanao hojiana juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kukubaliwa, hoja za hawa ni baat'ili mbele ya Mola wao Mlezi, na juu yao ipo ghadhabu, na itakuwa kwao adhabu kali.¹⁶

17. Mwenyezi Mungu ndiye aliye teremsha Kitabu kwa Haki, na Mizani. Na nini kitakacho kujuulisha ya kwamba pengine Saa ya Kiyama ipo karibu?¹⁷

18. Wasio amini huihimiza hiyo Saa ifike upesi; lakini wanao amini wanaiogopa, na wanajua kwamba hakika hiyo ni kweli. Ama kwa hakika hao wanao bishana katika khabari za hiyo Saa wamo katika upotofu wa mbali kabisa.¹⁸

19. Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake. Humruzuku ampendaye. Naye ni Mwenye nguvu, Mtukufu.¹⁹

20. Mwenye kutaka mavuno ya Akhera tutamzidishia katika mavuno yake, na mwenye kutaka mavuno ya duniani tutampa katika hayo, lakini katika Akhera hana fungu.²⁰

21. Au hao wana miungu ya kishirikina walio watungia dini asiyo itolea idhini Mwenyezi Mungu? Na lau lisinge kuwako neno la kupambanua basi wangeli katiwa hukumu baina yao. Na hakika wenye kudhulumu watapata adhabu chungu.²¹

22. Utawaona hao madhaalimu wanavyo kuwa na khofu kwa sababu ya waliyo yachuma, nayo yatawafika tu. Na walio amini na wakatenda mema watakuwamo katika mabustani ya Peponi. Humo watapata wayatakayo kwa Mola wao Mlezi. Hiyo ndiyo fadhila kubwa.²²

15 Basi kwa ajili ya umoja wa Dini, na kuondoa mtafaruku ndani yake, waite waishike Dini, na shikilia Wito huo kama alivyo kuamrisha Mwenyezi Mungu, wala usitafute kuyaridhi matamano ya washirikina. Na sema: Mimi naamrisha Vitabu vyote alivyo wateremshia Mwenyezi Mungu Mitume wake, na Mwenyezi Mungu ameniamrisha nisimamisha uadilifu baina yenu. Na waambie: Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wetu, na ndiye Muumba wenu. Vitendo vyetu ni vyetu sisi, si vyenu. Na vitendo vyenu ni vyenu nyinyi, si vyetu. Hapana la kubishana baina yetu na nyinyi, kwani haki iwazi. Mwenyezi Mungu atatukusanya kwa kutuhukumu kwa uadilifu. Na kwake Yeye peke yake ndio marejeo ya kurejea

16 Na hao wanao bisha katika mambo yaliyo khusu Dini ya Mwenyezi Mungu, baada ya watu kwisha uitikia Wito ulio wazi, ubishani wa watu hawa wenye shaka shaka ni baat'ili mbele ya Mola wao Mlezi. Na juu yao ipo ghadhabu kali kwa ukafiri wao. Na adhabu chungu inawangojea.

17 Mwenyezi Mungu ndiye aliye teremsha Kitabu cha Muhammad na viliyo kuwa kabla yake katika Vitabu vya Mitume, vyenye kukusanya Haki na uadilifu. Na nini cha kukujuvya, pengine wakati wa Saa ya Kiyama ipo karibu na wewe hujui.

18 Wanahimiza ije Saa ya Kiyama upesi upesi, kwa maskhara, hao wasio iamini. Na wenye kuiamini wamo katika khofu isitokee. Hao hawaihimizi. Na wanajua kuwa hiyo ni kweli iliyo thibiti, wala haina shaka. Naye *Subhanahu* anazindua kwamba hao wanao bisha kuja kwake bila ya shaka wamo katika upotovu ulio mbali na Haki.

19 Mwenyezi Mungu, ni mkuu wa kuwafanyia wema waja wake wote. Huwaruzuku awatakao kama anavyo taka. Naye ni Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye nguvu asiye shindika.

20 Mwenye kutaka kulipwa kwa a'mali yake thawabu za Akhera atalipwa mara mbili ujira wake. Na mwenye kutaka kwa a'mali yake starehe ya dunia tu, basi tutampa fungu lake hilo, na huko Akhera hatakuwa na fungu lolote la thawabu.

21 Kwani wao wanao miungu walio watungia dini nyengine asiyo iamrisha Mwenyezi Mungu? Hayakuwa hayo! Na lau halikwisha tangulia agano la kuakhirisha hukumu mpaka Siku ya Kiyama, basi bila ya shaka pangeli hukumiwa baina ya makafiri na Waumini hapa hapa duniani. Na hakika walio jidhulumu nafsi zao kwa ukafiri watapata adhabu yenye machungu makali.

22 Ewe unaye semezwa! Utawaona Siku ya Kiyama hao walio jidhulumu nafsi zao kwa ushirikina wamo katika khofu kuogopa malipo ya ushirikina wao, nayo yatawateremkia tu hapana hivi wala hivi. Na utawaona wenye kuamini na wakatenda mema wamestarehe katika mwahali mzuri kabisa katika Pepo.

23. Hayo ndiyo aliyo wabashiria Mwenyezi Mungu waja wake walio amini na wakatenda mema. Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi katika kujikurubisha. Na anaye fanya wema tutamzidishia wema. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mwenye shukrani.²³
24. Ati wanasema: Amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo? Mwenyezi Mungu akipenda atapiga muhuri juu ya moyo wako. Na Mwenyezi Mungu anaufuta upotofu na anaithibitisha Haki kwa maneno yake. Hakika Yeye anayajua yaliomo vifuani.²⁴
25. Naye ndiye anaye pokea toba kwa waja wake, na anasamehe makosa, na anayajua mnayo yatenda.²⁵
26. Na anawaitikia wanao amini na wakatenda mema, na anawazidishia fadhila zake. Na makafiri watakuwa na adhabu chungu.²⁶
27. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli wakunjulia riziki waja wake, basi bila ya shaka wangu pandi kiburi katika dunia. Lakini anaaiteremsha kwa kipimo akitakacho. Hakika Yeye anawajua vyema waja wake na anawaona.²⁷
28. Naye ndiye anaye iteremsha mvua baada ya wao kwisha kata tamaa, na hueneza rehema yake. Naye ndiye Mlinzi Mwenye kuhimidiwa.²⁸
29. Na katika Ishara zake ni kuumba mbingu na ardhi, na wanyama alio waeneza. Naye ni Mwenye uweza wa kuwakusanya apendapo.²⁹

Humo watapata neema wazitamaniazo kwa Mola wao Mlezi. Hayo ndiyo malipo makubwa, na ndio fadhila kubwa ya kutarajiwa.

23 Hiyo fadhila kubwa ndiyo ambayo Mwenyezi Mungu amewabashiria waja wake Waumini, wat'iifu. Ewe Mtume! Sema: Mimi sitaki kwenu ujira kwa kufikisha huu Ujumbe, isipo kuwa mumpende Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika kujikurubisha kwenu kwake Yeye *Subhanahu*, kwa vitendo vyema. Na mwenye kutenda ut'iifu Mwenyezi Mungu atampa ujira mara mbili. Hakika Mwenyezi Mungu ni mkunjufu wa maghfira kwa wenye madhambi, ni Mwenye shukrani kwa waja wake wenye vitendo vyema.

24 Je! makafiri wanasema Muhammad anamzulia uwongo Mwenyezi Mungu? Mwenyezi Mungu akipenda atakufungia moyo wako usubiri maudhi yao, na tuhuma yao kuwa unamzulia Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ataondoa na ataushinda ukafiri na ataupa nguvu Uislamu na ataudhihirisha kwa wa'hyi alio mteremshia Mtume wake s.a.w., kwani - Yeye- Mwenyezi Mungu anajua yote yaliomo ndani ya nyoyo zenu nyote.

25 Ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kupokea toba kwa watu wanao mt'ii hata kwa makosa yaliyo zaidi kuliko yale wanayo ombea toba. Na Yeye ndiye anaye samehe madhambi yote isipo kuwa shirki, kwa kufadhili na kurehemu; na anayajua myatendayo ikiwa ya kheri au shari.

26 Na huwaitikia Waumini kwa wanayo yaomba, na huwazidishia juu ya hayo wanayo yaomba. Na makafiri watapata adhabu yenye kufikia ukomo wa ukali na uchungu.

27 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli wakunjulia waja wake wote, kama watakavyo, basi bila ya shaka wangu pandi kiburi katika ardhi wakafanya dhulma. Lakini Mwenyezi Mungu humkunjulia riziki amtakaye, na humdhikisha amtakaye, kwa mujibu wa hikima yake. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua vyema mambo yote ya waja wake, ya siri na dhaahiri. Basi Yeye humkadiria kila mmoja kwa linalo msilahi kwa mujibu wa hikima yake.

28 Na Mwenyezi Mungu, peke yake, ndiye anaye iteremsha mvua inayo waokoa na ukame baada ya kwisha kata tamaa na kuzidi kiangazi, kuwa ni rehema kwa waja wake. Na Yeye hueneza baraka za mvua katika mimea, na miti ya matunda, na wanyama, na nyanda, na milima. Na Yeye, peke yake, ndiye Mwenye madaraka ya kuyapanga mambo yote ya waja wake, na ndiye wa kuhimidiwa kwa neema zake, na vitendo vyake vyote.

29 Na katika dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu kuumba atakacho ni huku kuumba mbingu na ardhi kwa nidhamu iliyo pangwa; na kuumbwa vilivyo tenganihwa humo na kuenezwa wanayama wanao onekana na wengineo. Na Mwenyezi Mungu aliye hakikisha uweza wake kwa kuumba hivyo vilio tajwa ni Muweza wa kuwakusanya wote katika wakati autakao kuwafufulia kwa ajili ya malipo.

30. Na misiba inayo kusibuni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu. Naye anasamehe mengi.³⁰
31. Na nyinyi hamwezi kushinda katika ardhi. Na wala nyinyi hamna mlinzi wala msaidizi badala ya Mwenyezi Mungu.³¹
32. Na katika Ishara zake ni vyombo vinavyo kwenda na kurejea baharini kama vilima.³²
33. Akitaka, huutuliza upepo navyo hivyo vyombo husimama tutwe juu ya bahari. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa kila mwenye kusubiri akashukuru.³³
34. Au huviangamiza hivyo vyombo kwa sababu ya waliyo yatenda hao watu. Naye husamehe mengi.³⁴
35. Na ili wajue wanao jadiliana katika Ishara zetu kwamba hawana pahala pa kukimbilia.³⁵
36. Basi vyote mlivyo pewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora, na cha kudumu kwa ajili ya walio amini, na wakawa wanamtegemea Mola wao Mlezi.³⁶
37. Na wanayo yaepuka madhambi makubwa na mambo machafu, na wanapo kasirika wao husamehe,³⁷
38. Na wanao mwikitia Mola wao Mlezi, na wakashika Sala, na mambo yao yakawa ni kwa kushauriana baina yao, na kutokana na tulicho waruzuku wakawa wanatoa,³⁸
39. Na ambao wanapo fanyiwa jeuri hujitetea.³⁹

30 Na msiba wowote unao kusibuni mnao uchukia ni kwa sababu ya maasi yenu. Na anayo yasamehe Mwenyezi Mungu duniani au akayachukulia ahadi humo, basi Mwenyezi Mungu ni Karimu; hatokuwa tena wa kuadhibu kwa hayo Akhera. Na Kwa hivi ametakasika na dhulma, na amesifika kwa rehemu kunjufu.

31 Wala nyinyi hamwezi kumshinda Mwenyezi Mungu na kumzuilia asilete masaibu duniani kuwa ni adhabu kwa ajili ya maasi yenu, na hata mkikimbia vipi. Na wala hamna asiye kuwa Mwenyezi Mungu wa kukurehemuni pindi ikikuteremkieni balaa, wala hamna wa kukunusuruni nayo.

32 Na katika dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu, ni majahazi yaendayo katika bahari kama vilima virefu kwa ukubwa wake.

33 Mwenyezi Mungu akipenda huutuliza upepo kukawa shuwari; basi majahazi yaliyo thibiti juu ya bahari hutulia hayendi huko yendako. Hakika huko kwenda kwao na kusimama kwao kwa amri ya Mwenyezi Mungu ni dalili wazi juu ya uweza wa Mwenyezi Mungu. Wanayazingatia hayo Waumini wenye kusubiri wakati wa dhiki, na wenye kushukuru wakati wa furaha.

34 Au akayateketeza hayo majahazi kwa sababu ya madhambi ya walio panda, kwa kuwapelekea upepo wa kimbunga. Na Mwenyezi Mungu akipenda anasamehe mengi; kwa kuwa hawaadhibu kwa kuzuia upepo na kuleta shuwari, au kwa kuleta kimbunga cha kuwazamisha.

35 Mwenyezi Mungu, *Subhanahu*, hufanya hayo ili Waumini wapate kuzingatia, na wajue wale wanao zirudi Ishara zake kwa upotovu kwamba wao wamo katika mkono wake, wala hawana pa kuikimbia adhabu yake.

36 Msidanganyike na starehe za dunia. Kwani enyi watu! Yote mliyo pewa, mali, wana, na vyenginevyo, ni starehe zenu za maisha ya duniani. Na aliyo yaandaa Mwenyezi Mungu katika neema za Peponi ni bora na zinadumu zaidi kwa wenye kuamini, na kumtegemea Muumba wao na Mlezi wao wa pekee;

37 Na wanao jitenga mbali na kupanda madhambi makubwa makubwa aliyo yakataza Mwenyezi Mungu, na madhambi yote yaliyo zidi ubaya, na pindi wakichochea kwa kufanyiwa mabaya katika mambo ya dunia yao, wao wenyewe wakawa mbele kuanza kusamehe ili kuleta masikilizano;

38 Na wanao uitikia wito wa Muumba wao na Mlezi wao, na wakamuamini, na wakazihifadhi Sala zao, na ukawa mwendo wao ni kushauriana katika mambo yao ili upatikane uadilifu katika jamii zao, bila ya mtu mmojapo au kikundi cha wachache kutaka kuwatumilia mabavu wengine, na wakawa wanatoa kwa njia za kheri kutokana na neema alizo mneemesha Mwenyezi Mungu;

39 Na wale ambao anapo wavamia mwenye kudhulumu wao wanajitetea nafsi zao kuupinga ule uvamizi

40. Na malipo ya uovu ni uovu mfano wa huo. Lakini mwenye kusamehe, na akasuluhisha, basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye hawapendi wenye kudhulumu.⁴⁰

41. Na wanao jitetea baada ya kudhulumiwa, hao hapana njia ya kuwalaumu.⁴¹

42. Bali lawama ipo kwa wale wanao wadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Hao watapata adhabu iliyo chungu.⁴²

43. Na anaye subiri, na akasamehe, hakika hayo ni katika mambo ya kuazimiwa.⁴³

44. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha kupotea, hana mlinzi baada yake. Na utawaona wenye kudhulumu watakapo iona adhabu wanasema: Je! Ipo njia ya kurudi?⁴⁴

45. Na utawaona wanapelekwa kwenye Moto, nao wamenyenyekea kwa unyonge, wanatazama kwa mtazamo wa kificho. Na walio amini watasema: Hakika wapatao khasara ni hao walio khasiri nafsi zao na ahali zao Siku ya Kiyama. Ama hakika wenye kudhulumu watakuwa katika adhabu ya daima.⁴⁵

46. Wala hawatakuwa na walinzi wa kuwanusuru mbele ya Mwenyezi Mungu. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemwacha kupotea, hana njia yoyote.⁴⁶

47. Muitikieni Mola wenu Mlezi kabla haijafika siku isiyo epukika itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Siku hiyo hamtakuwa pa kukimbilia wala hamtakuwa na cha kukingia.⁴⁷

wake.

40 Na malipo ya mwovu, ni kumtendea uovu kama wake, kwa kufuata uadilifu. Lakini mwenye kusamehe uovu alio tendewa, naye anaweza kulipiza, na akaleta masikilizano baina yake na yule khasimu yake, kwa kujenga mapenzi, basi thawabu zake ziko kwa Mwenyezi Mungu. Hapana anaye zijua kadiri yake isipo kuwa Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu hawarehemu wavamizi wanao fanya uadui katika haki za watu, kwa kuzikiuka sharia za Mwenyezi Mungu.

41 Hakika wanao wapa adhabu wavamizi kama wanavyo fanya uadui wao, hao hawaingiliwi wala hawalaumiwi.

42 Bali lawama na kushikwa haki ni juu ya wanao fanya uadui, wakadhulumu watu, na wakafanya kiburi katika nchi, na wakafisidi humo bila ya haki. Hao watapata adhabu yenye uchungu mkali.

43 Ninaapa: Bila ya shaka, mwenye kuvumilia kudhulumiwa, akamwachilia aliye mdhulumu, wala asiitete nafsi yake, pindi ikiwa huko kusamehe kwenyewe hakuupalili ufsadi ukapata nguvu katika nchi, hakika hayo ni katika mambo ambayo yanatakikana mwenye akili ajilazimishe kuyatenda.

44 Na mwenye kuiptea Njia ya Uwongofu kwa kuwa hana ujuzi mwema, basi hana wa kumnusuru isipo kuwa Mwenyezi Mungu, ndiye wa kumwongoa na wa kumkinga na adhabu. Na, ewe unaye semezwa! Utaona Siku ya Kiyama wale wenye kudhulumu watakapo iona adhabu ya Akhera wanamuuliza Mola wao Mlezi, watumie mbinu gani wapate kurejea duniani, ili wapate kutenda mema, siyo waliyo kuwa wakiyatenda kwanza?

45 Na kadhaalika, utawaona walio dhulumu, wakipelekwa Motoni, wamenywea kwa sababu ya unyonge ulio tokana na hivyo vitisho walivyo vikuta, wakitupia jicho kwa kificho kwenye huo Moto kwa kuukhofu vituko vyake. Na hapo Waumini watasema: Hakika walio khasiri kweli ni hao walio dhulumu nafsi zao kwa ukafiri wao, na wakawakhasiri wake zao na watoto wao na jamaa zao kwa mfarakano walio usabibisha baina yao. Na Mwenyezi Mungu ananabihisha kwamba wenye kudhulumu watakuwa katika adhabu ya milele.

46 Na wala hawatakuwa wa kuwanusuru kutokana na ile miungu ya uwongo walio kuwa wakiiabudu badala ya Mwenyezi Mungu, na walio kuwa wakiiit'ii katika kumuasi Mwenyezi Mungu, waje kuwaokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kupotea Njia ya Haki kwa kuto kuwa na ujuzi, basi hatokuwa na njia ya kumwokoia na mwisho muovu.

47 Enyi watu! Kimbilieni kuitikia aliyo kuitieni Mtume wa Mwenyezi Mungu aliye kuumbeni na akakuleeni, nayo ni Imani na Ut'iifu, kabla uhai haujamaliza fursa ya kutenda vitendo, na ikafika Siku ya Hisabu ambayo Mwenyezi Mungu hairudishi nyuma tena baada ya kwisha ihukumia. Siku hiyo

48. Na wakipuuzwa, basi Sisi hatukukupeleka ili uwe mwangalizi wao. Si juu yako ila kufikisha Ujumbe tu. Na hakika Sisi tukimwonjesha mtu rehema kutoka kwetu, huifurahia. Na akisibiwa na ovu kwa sababu ya iliyo yatanguliza mikono yao, basi hakika mtu huyu anakufuru.⁴⁸

49. Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; anaumba apendavyo, anamtunukia amtakaye watoto wa kike, na anamtunukia amtakaye watoto wa kiume,⁴⁹

50. Au huwachanganya wanaume na wanawake, na akamfanya amtakaye tasa. Hakika Yeye ni Mjuzi Mwenye uweza.⁵⁰

51. Na haikuwa kwa mwanaadamu kwamba Mwenyezi Mungu amsemeze ila kwa Wahyi (Ufunuo), au kwa nyuma ya pazia, au kumtuma Mjumbe. Naye humfunulia ayatakayo kwa idhini yake. Hakika Yeye ni Mtukufu, Mwenye hikima.⁵¹

52. Na namna hivi tumekufunulia Qur'ani kwa amri yetu. Ulikuwa hujui Kitabu ni nini, wala Imani. Lakini tumekifanya kuwa ni Nuru ambayo kwayo tunamwongoa tumtakaye katika waja wetu. Na hakika wewe unaongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka.⁵²

53. Njia ya Mwenyezi Mungu ambaye ni vyake Yeye tu viliomo mbinguni na katika ardhi. Jueni kuwa mambo yote yanarudi kwa Mwenyezi Mungu.⁵³

hamtakuwa na pa kukimbilia pa kukuhamini na adhabu, wala hapana cha kuzuia kitakacho kufikieni.

48 Wakipuuzwa washirikina kukuitikia wewe, ewe Mtume, basi usihuzunike. Kwani wewe si mwangalizi wao kwa hayo wanayo yatenda. Wewe umelazimishwa kufikisha Ujumbe tu, na hayo umeyabainisha wazi. Na tabia ya watu tukiwapa wasaa hupanda kiburi. Na ukiwasibu msiba kwa sababu ya maasi yao, mara wanasahau neema, wanahuzunika kwa kuteremkiwa na balaa, na wanaingia katika kufuru.

49 Ni wa Mwenyezi Mungu peke yake Ufalme wa mbingu na ardhi, kwa kuumba, kuudabiri, na kuusarifu. Yeye anaumba atakacho. Humtunukia amtakaye wana wa kike, na akamtunukia amtakaye wana wanaume bila ya wanawake.

50 Na Yeye *Subhanahu* humfadhili amtakaye kwa kumchanganyia wanaume na wanawake, na akamfanya amtakaye bila ya mtoto yeyote. Hakika Mwenyezi Mungu anajua vyema kila kitu. Ni Muweza wa kutenda kila akitakacho.

51 Wala haimfalii mtu kusemezwa na Mwenyezi Mungu ila iwe kwa Wahyi (Ufunuo) kwa kumtilia ilhamu katika moyo wake, au usingizini, au kwa kusikia maneno ya Kiungu bila ya kumwona Asemaye, au kwa kutumwa Malaika akaonekana sura yake, na akasilizana sauti, akamfunulia Nabii kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kama atakayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtenda nguvu, basi haziwiliki Mwenye kupita ukomo hikima yake katika kuendesha mambo yake na kupanga kwake.

52 Na kama tulivyo wafunulia Mitume kabla yako, basi tumekufunulia nawe, ewe Mtume, hii Qur'ani ili ihuise nyoyo kwa amri yetu. Kabla ya kuletewa wewe hii ulikuwa hujui nini Qur'ani, wala hujui Sharia za Imani. Lakini tumeifanya Qur'ani kuwa ni Nuru Kubwa ya kuwaongoza wenye kukhiari Uwongofu. Na wewe bila ya shaka utakuwa ukiwaitia watu kwa hii Qur'ani kwenye Njia Iliyo Nyooka.

53 Njia ya Dini ya Mwenyezi Mungu ambaye ndiyo vyake Yeye tu peke yake, vyote viliomo mbinguni na katika ardhi, kwa kuumba, na kupanga, na kuendesha. Naye ananabihisha, *Subhanahu*, kwamba kwake Yeye peke yake ndio yanarejea mambo yote.

Sura 43 - Azzukhruf

Utangulizi

Imeanzia Sura hii kwa harufi mbili za alifbete, na ikafuatia kwa kuitaja Qur'ani na kueleza cheo chake kwa Mwenyezi Mungu. Kisha Sura ikaingia kubainisha msimamo wa wale wanao zifanyia maskhara Risala za Mitume wao, na ikazileta dalili nyingi za kuthibitisha Imani ya Mwenyezi Mungu pekee. Na juu ya hoja hizo wao wakamzulia Mwenyezi Mungu kuwa ana washirika, na wakamfanya kuwa ana watoto wa kike, na wao wanao wa kiume. Na walipo ishiwa na hoja wakashikilia mila za baba zao.

Kisha Sura ikasimulia kisa cha Ibrahim, na ikafuutiliza kule kuyaona makuu makafiri wa Makka ya kwamba Qur'ani iliteremka juu ya Muhammad, wala isiteremke juu ya mmoja katika wakuu wa miji yao miwili. Hayo ni kama kwamba wao ndio wanao zigawanya fadhila za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu alikwisha wagawia maisha yao ya duniani, kwa kuwa wao wenyewe wameshindwa hayo. Kisha Sura ikathibitisha kwamba lau kuwa si kuchukia wasije watu wote wakakufuru basi bila ya shaka angeli mpa kafiri starehe na mapambo na uzuri wote wa duniani. Kadhaalika Sura imebainisha kwamba mwenye kupuuzia Haki Mwenyezi Mungu humsalitisha na Shet'ani amwongoze kwenye maangamio. Kisha Sura inasimulia kisa cha Musa na Firauni, na alivyo ghurika Firauni na ufalme wake, na yaliyo mteremkia Firauni na kaumu yake ya mateso ya Mwenyezi Mungu. Na hayo akafuatiwa kutajwa Bin Maryamu, na kwamba yeye ni mja aliye neemeshwa na Mwenyezi Mungu, na akawaita watu wende kwenye Njia Iliyo Nyooka. Na baada ya kuonya kwa adhabu ya Siku ya Kiyama itayo wapata walio dhulumu, na kubashiriwa Waumini kuwa watapata Pepo ambayo ndani yake macho yao yatatua, Sura inakhitimisha kueleza kuwa Ufalme wa Mwenyezi Mungu umeenea kote, na hao walio washirikisha naye hawanalo wawezalo. Basi, ewe Muhammad! Wapuuzilie mbali, na useme: Salamu! Watakuja jua

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. H'a Mim¹

2. Naapa kwa Kitabu kinacho bainisha.²

3. Hakika Sisi tumeifanya Qur'ani kwa Kiarabu ili mfahamu.³

4. Na hakika hiyo imo katika Asili ya Maandiko yalioko kwetu, ni tukufu na yenye hikima.⁴

1 H'a Mim:- Imeanza Sura hii kwa baadhi ya harufi za kutamkwa kama ilivyo ada ya Qur'ani katika kuanzishia Sura nyingi kwa harufi kama hizi.

2 Mwenyezi Mungu, *Subhanahu*, anaapa kwa Qur'ani inayo eleza wazi yale iliyo yakusanya katika mambo ya itikadi na hukumu.

3 Hakika Sisi tumeijaalia Qur'ani iwe kwa lugha ya Kiarabu, ili mweze kuelewa umuujiza wake, na mweze kuzingatia maana zake.

4 Na hakika hii Qur'ani iliyo thibiti katika *Lauhun Mahfuudh*, Ubao ulio hifadhiwa, ulioko kwetu, bila ya shaka, ina cheo cha juu, na imepangwa kwa mpango wa hikima, katika mwisho wa ufasihi. (Vitabu vyote vya mbinguni asili yake anayo Mwenyezi Mungu, katika Ujuzi wake wa tokea azali, *Al- I'Imu al-azaliy* au Ubao Ulio Hifadhiwa *Al-lauhu al-mahfuudh* au Asili ya Maandiko *Ummu-l-kitabi*. Kwa sababu ya

5. Je! Tuache kukukumbusheni kabisa kwa kuwa nyinyi ni watu mlio pita mipaka kwa ukafiri?⁵
6. Na Manabii wangapi tuliwatuma kwa watu wa zamani!⁶
7. Na hawajii Nabii yeyote ila walikuwa wakimkejeli.⁷
8. Na tuliwaangamiza walio kuwa na nguvu kushinda wao. Na mfano wa watu wa zamani umekwisha pita.⁸
9. Na ukiwauliza: Nani aliye ziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Kaziumba Mwenye nguvu, Mjuzi,⁹
10. Ambaye amekufanyieni ardhi kama tandiko, na akakufanyieni ndani yake njia mpate kuongoka.¹⁰
11. Na ambaye ndiye aliye teremsha kutoka mbinguni maji kwa kiasi, na kwa hayo tukaifufua nchi iliyo kufa. Na namna hivi ndivyo mtakavyo tolewa.¹¹
12. Na ambaye ndiye aliye umbwa katika kila kitu jike na dume, na akakufanyieni marikebu na wanyama mnao wapanda.¹²
13. Ili mkae vizuri migongoni mwao, kisha mkumbuke neema za Mola wenu Mlezi mnapokaa sawa sawa juu yao na msembe: Ametakasika aliye mfanya huyu atutumikie, na tusingeli weza kufanya haya wenyewe.¹³

kuwa Vitabu vilivyo kuja zamani, ikiwa Taurati, Zaburi, Injili n.k. vilikuwa ni vya muda fulani, na kwa mataifa fulani, basi haikuwepo dharura vibaki kwa usafi kila neno lake. Ni makusudio yake tu yabakie, yaliyo kuwa ya msingi. Ama ilipo fika wakati wa kudumisha Ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa zama zote, na kwa watu wote, ndio ikaja Qur'ani ambayo imehifadhiwa kila neno lake. Na ndio siri ya kuletwa kwa lugha ya Kiarabu na ikalindwa kwa lugha ile, ijapo kuwa itatarajumiwa katika lugha nyengine. Mzozano wowote unao tokea unarejzwa kwenye asli ile ya Kiarabu ambayo haikubadilika hata chembe, wala haitabadilika mpaka Siku ya Kiyama. Huo peke yake ni muujiza. Ama vitabu vya Biblia ni kama maji yaliyo tibuliwa na ng'ombe mpaka kwenye chemchem yake. Chemchem ya Qur'ani haikutibuliwa. Ijapo kuwa wanyama na watu wanaweza kunywa maji yake huku chini, kwenye kitovu cha chemchem hakuguswi. Huko ni kwenye Qur'ani hiyo ya Kiarabu, safi kama ilivyo kwenye Ubao Ulio Hifadhiwa.)

5 Je! Tukupeni muhula, tuache kukuteremshieni Qur'ani kwa kukutupilieni mbali, kwa sababu ya kupita kwenu mipaka ya ukafiri juu ya nafsi zenu? Hayawi hayo, kwa kufuata hukumu ya kulazimikana kwenu na hoja.

6 Nasi tuliwatuma Manabii wengi kuyaendea mataifa yaliyo tangulia, basi hapana ajabu kitu kumtuma Mtume kwenu.

7 Wala hawajii Mtume yeyote kuwakumbusha Haki ila huendelea na kumfanyia maskhara.

8 Basi tuliwateketeza walio kadhibisha walio tangulia; na hao walikuwa wamewazidi makafiri wa Makka kwa nguvu na ushupavu. Basi wasidanganyike hawa na ujabari wao. Na zilikwisha tangulia katika Qur'ani hadithi za ajabu za watu wa kale, za kuwafanya wenginewe wazingatie. Basi enyi mnao kanusha! Zingatieni.

9 Na ninaapa, ewe Mtume! Ukiwauliza makafiri nani aliye ziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema kuyajibu hayo: Mwenyezi Mungu ndiye aliye ziumba, ambaye anasifika kwa hakika ya mambo kuwa ni Mwenye nguvu, ni Mwenye Ujuzi ulio enea.

10 Ambaye amekufanyieni ardhi ni pahala palipo tanda, ili muweze kukaa humo na mjitumilie, na akakufanyieni ndani yake njia mnazo zipitia katika safari zenu mpate kufikia mtakako.

11 Na ambaye aliye kuteremshieni maji kwa kiasi ya haja kutoka mbinguni tukaihuisha nchi kavu isiyoyana mimea. Kuhuisha kama huko ndivyo mtavyo fufuliwa kutoka makaburini kwenu kwa ajili ya hisabu. Basi yawaje mnakukataa?

12 Na ambaye aliye kuumbieni namna zote za viumbe, akavifanya vikutumikieni vyombo vya baharini na ngamia kuwa ni vipando katika safari zenu kutimiza haja zenu.

13 Ili mtulie juu yao, kisha mkumbuke neema za Muumba wenu na Mlezi wenu kwa kuvifanya hivyo vikutumikieni mnapo tulia juu yao, na kwa kuadhimisha kule kuvifanya vinyonge kwa njia ya ajabu, na kutambua uweza mlio wezeshwa kuvidhibiti na kuvitawala, msembe: Subhana, Ametakasika aliye mfanya

14. Na hakika sisi tutarudi kwa Mola wetu Mlezi.¹⁴
15. Na wanamfanyia katika waja wake fungu. Kwa hakika mwanaadamu ni mtovu wa fadhila aliye dhaahiri.¹⁵
16. Au amejichukulia watoto wanawake katika vile alivyo viumba, na akakuteulieni nyinyi watoto wanaume?¹⁶
17. Na anapo bashiriwa mmoja wao kwa yale aliyo mpigia mfano Mwenyezi Mungu, uso wake husawijika na hujaa hasira.¹⁷
18. Ati aliye lelewa katika mapambo, na katika mabishano hawezi kusema kwa bayana?¹⁸
19. Na wakawafanya Malaika, ambao ni waja wa Mwingi wa Rehema, ni wanawake! Kwani wameshuhudia kuumbwa kwao? Ushahidi wao utaandikwa na wao watahojiwa!¹⁹
20. Nao husema: Angeli penda Mwingi wa Rehema tusingeli waabudu sisi. Hawana ujuzi wowote wa hayo! Hawana ila kusema uwongo tu!²⁰
21. Kwani tuliwapa Kitabu kabla ya hichi, na ikawa wao wanakishikilia hicho?²¹
22. Bali wanasema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, basi na sisi tunaongoza nyayo zao.²²
23. Na kadhaalika hatukumtuma mwonyaji kwenye mji wowote ila watu wake walio deka kwa starehe walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao.²³
24. Akasema (Mwonyaji): Hata nikikuleteeni yenye uwongofu bora kuliko mliowakuta

huyu (au hichi) kuwa dhalili kututumikia na sisi wenyewe tusingeli weza kumdhalisha.

14. Na hakika sisi ni wenye kurejea kwa Muumba wetu baada ya maisha haya, ili ahisabiwe kila mmoja kwa iliyo tanguliza mikono yake.

15. Na makafiri washirikina wamemfanyia Mwenyezi Mungu *Subhanahu* katika viumbe vyake mwana wakaamini kuwa ni sehemu ya nafsi yake. Hakika mwanaadamu kwa kitendo chake hichi hadi amepita ukomo katika ukafiri wake, na upinzani wake uwazi.

16. Ati mnadai kwamba Yeye amejitwalia katika viumbe vyake watoto wa kike, na nyinyi akakukhiarieni watoto wanaume? Ama hakika haya ni mambo ya ajabu kweli!

17. Wamekuzulia Wewe hayo, na ilhali wao akipewa khabari mmoja wao kwamba amepata mtoto wa kike uso wake husawajika kwa kuudhika, naye kaja masikitiko na huzuni kwa kuona anapewa khabari mbaya.

18. Hivyo hawa wana fanya jeuri ya kumpachikia Mwenyezi Mungu mwana, ambaye kwa maumbile yake amelelewa katika mapambo, na hata hawezi kujadiliana na kupambana kwa hoja kwa nuksani yake ya kubaini. Ama hili ni jambo la ajabu!

19. Na ati wakawaita Malaika, viumbe vya Mwenyezi Mungu, kuwa ni wanawake. Kwani wao waliwashuhudia walipo umbwa, hata watoe hukumu kwa jambo hilo? Hawakuliona! Sisi tutasajili uzushi wao huu. Na Siku ya Kiyama watakuja hisabiwa.

20. Na washirikina husema ati: Lau kuwa Mwingi wa Rehema angeli kuwa anataka tusiibudu hii miungu basi tusingeli iabudu. Wanakusudia kudai kuwa ati Mwenyezi Mungu yu radhi kuabudiwa hiyo miungu. Wanasema hayo bila ya kuwa na ilimu yoyote ya kuyategemezea wayasemayo. Hawa si chochote ila ni wenye kudhani tu. Hunena maneno yasio na ushahidi wowote.

21. Kwani tuliwapa Kitabu kabla ya Qur'ani cha kuunga mkono huu uzushi wao, ndio maana wakashikamana nao kwa nguvu hivi? Hatukuwateremshia Kitabu namna hiyo. Basi hawana hoja ya kuinukulu.

22. Lakini washirikina walipo shindwa na hoja zote walisema: Hakika sisi tumewakuta baba zetu wakifuata dini hii; na sisi tunaendelea kufuata nyayo zao.

23. Mfano wa hali ya watu hawa ni mfano wa mataifa yaliyo tangulia. Hatukumtuma Mtume yeyote kwenye mji kabla yako ila walisema wale wenye kuneemeka katika huo mji, nao ndio walio takabari kwa hizo neema: Hakika sisi tumewakuta baba zetu wakifuata dini hii, basi ndio sisi tunakwenda mwendo wao. Basi kufuata kijinga ni upotovu wa tangu kale.

nao baba zenu? Wakasema: Sisi tunayakataa tu hayo mliyo tumwa.²⁴

25. Basi tukawalipizia. Angalia ulikuwaje mwisho wa walio kadhibisha!²⁵

26. Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu,²⁶

27. Isipo kuwa yule aliye niumba, kwani Yeye ataniongoa.²⁷

28. Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee.²⁸

29. Bali tuliwastarehesha hawa na baba zao mpaka ikawafikia Haki na Mtume aliye bainisha.²⁹

30. Na ilipo wafikia Haki wakasema: Huu ni uchawi, na sisi hakika tunaukataa.³⁰

31. Na walisema: Kwa nini Qur’ani hii haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii?³¹

32. Kwani wao ndio wanao gawa rehema za Mola wako Mlezi? Sisi tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na tukawanyanyua baadhi yao juu ya wengine kwa daraja nyingi; kwa hivyo baadhi yao wanawafanya wengine wawatumikie. Na rehema za Mwenyezi Mungu ni bora kuliko hayo wanayo yakusanya.³²

33. Na lau isinge kuwa watu watakuwa kundi moja tungeli wajaalia wanao mkufuru Rahmani wana nyumba zao zina dari ya fedha, na ngazi zao pia wanazo pandia,³³

34. Na milango ya nyumba zao na vitanda wanavyo egemea juu yake,³⁴

24 Mwonyaji akasema: Je! Mnafuata baba zenu hata nikikujieni na yaliyo elekea zaidi kukupelekeni kwenye uwongofu kuliko mlio wakuta nao baba zenu? Wakasema kuwajibu Mitume wao wakiwakadhibisha kwa Dini: Sisi tunayakataa yote mliyo tumwa kutuambia!

25 Basi tukawatesa walio wakadhibisha Mitume wao kwa mateso makali katika dunia. Basi hebu angalia, ewe mwenye kuzingatia, vipi ulikuwa mwisho wa wenye kukukadhibisheni kuwa ni mfano wa ajabu, na mawaidha makubwa!

26 Na ewe Muhammad! Waambie hao wanao kanusha hadithi ya Ibrahim pale alipo mwambia baba yake: Hakika mimi nimejitenga mbali na ibada ya kuiabudu hii miungu yenu ya uwongo.

27 Lakini mimi namuabudu Mwenyezi Mungu aliye niumba; kwani ni Yeye ndiye atakaye niongoza kwendea Njia ya Haki.

28 Kwa kuwatangazia hivyo, likawa hilo Neno la Tawhidi, ni neno lenye kubakia katika dhuriya zake, ili wapate kulirejelea, waliamini.

29 Washirikina hawakutimiza matumaini ya Ibrahim, wala Mimi sikuwapatiliza papo kwa papo, bali nimewastarehesha hawa ulio nao, ewe Muhammad, na niliwastarehesha baba zao kabla yao kwa namna mbali mbali za neema, mpaka ilipo teremka Qur’ani kuwaitia Haki, na akawajia Mtume mwenye kubaini wazi akiwaita.

30 Na ilipo teremka Qur’ani kuwaongoza kwenye Tawhid wakaongeza juu ya ushirikina wao kuita Qur’ani : “uchawi” na “kiini macho”, kwa kejeli. Na wakashikilia ukafiri wao.

31 Na washirikina, kwa kumdharau Muhammad na kuona haiwezi kuwa yeye ateremshiwe Qur’ani, walisema: Kwa nini basi hii Qur’ani, ambayo yeye anadai kuwa ni Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, asiteremshiwe mtu mkubwa mtukufu katika watu wa Makka au T’aif?

32 Funguo za Utume hazimo katika mikono ya washirikina, hata wao wawakabidhi watu wenye vyeo. Sisi tumewapangia maisha yao kwa kuwa wao wenyewe hawajiwezi. Na tumewafadhilisha baadhi juu ya wengine katika riziki na vyeo, na kwa hivyo baadhi yao huwafanya wengineo wawasaidie na wawatumikie katika kutimiza haja zao, ili wategemeane katika kutafuta maisha na kupanga uhai. Na Unabii na yaliyo khusiana nayo katika neema za Akhera na dunia, ni bora kuliko vyeo vyote vya duniani.

33 Na lau kuwa si karaha ya kuwa watu wote wawe makafiri wakiona makafiri wamo katika nafasi ya riziki, basi tungeli wafanyia wanao mkufuru Mwenyezi Mungu kuwa nyumba zao ziwe na dari za fedha, na pia ngazi za nyumba zao, kwa kuwa hayo hayana thamani kitu mbele yetu.

34 Na tungeli wafanyia milango ya nyumba zao na vitanda kuwa ni vya fedha wakineemeka navyo na wakiegemea juu yake. Na tungeli wafanyia mapambo ya kila kitu. Na starehe zote hizo tulizo kusifia

- 35.** Na mapambo. Lakini hayo si chochote ila ni starehe ya maisha ya dunia tu, na Akhera iliyoko kwa Mola wako Mlezi ni ya wenye kumchamngu.³⁵
- 36.** Anaye yafanyia upofu maneno ya Rahmani tunamwekea Shet'ani kuwa ndiye rafiki yake.³⁶
- 37.** Na hakika wao wanawazuilia Njia na wenyewe wanadhani kuwa wameongoka.³⁷
- 38.** Hata atakapo tujia atasema: Laiti ungeli kuwako baina yangu na wewe kama umbali baina ya mashariki na magharibi. Rafiki mwovu mno wewe!³⁸
- 39.** Na kwa kuwa mlidhulumu, haitakufaeni kitu leo kwamba nyinyi mnashirikiana katika adhabu.³⁹
- 40.** Je! Unaweza kuwasikilizisha viziwi, au unaweza kuwaongoa vipofu na waliomo katika upotofu ulio wazi?⁴⁰
- 41.** Na hata tukikuondoa, Sisi tutalipiza kisasi chetu kwao.⁴¹
- 42.** Au tutakuonyesha tulio waahidi. Nasi bila ya shaka tuna uweza juu yao.⁴²
- 43.** Basi wewe yashike yaliyo funuliwa kwako. Hakika wewe uko kwenye Njia Iliyo Nyooka.⁴³
- 44.** Na hakika haya ni ukumbusho kwako na kwa kaumu yako. Na mtakuja ulizwa.⁴⁴
- 45.** Na waulize Mitume wetu tulio watuma kabla yako: Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Rah'mani?⁴⁵

si chochote ila ni starehe za kupita njia, ni za uhai huu tu wa duniani. Na malipo ya Akhera mbele ya Muumba wako na Mlezi wako yameandaliwa kwa wanao jilinda na ushirikina, na wakayaepuka maasi ya kuangamiza.

35 Tazama tanbihi ya 34.

36 Na mwenye kujitia upofu na Qur'ani aliyotekemsha Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kuwa ni kumbusho kwa walimwengu wote, tunamsalitisha na Shetani, anakuwa naye daima, akimpoteza na akimzuzua.

37 Na hakika Mashetani wanao jitia upofu na Qur'ani huwazuia na Njia anayo itia Rahmani. Na hao wanao tumiliwa wanadhani kwa kuwafuata rafiki zao kwamba wao wamo katika uwongofu.

38 Hata yule aliye jipa upofu na Qur'ani atapo fika kwa Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama, na akaona matokeo ya kule kujitia kwake upofu, atamwambia rafiki yake kwa majuto: Laiti wewe nami tungeli kuwa mbali mbali duniani umbali wa mashariki na magharibi! Ama wewe ulikuwa sahibu muovu mno kwangu, mpaka umekuja nitumbukize katika shimo la Moton!

39 Na hapo wataambiwa kwa kuwahizi: Leo hamtapunguziwa adhabu, kwani mmejidhulumu wenyewe kwa ukafiri wenu, kwa sababu mlishirikiana na mashetani wenu. Kwani kila mmoja anateseka kwa adhabu ya kumtoshia mwenyewe.

40 Je! Unaweza kumwongoa aliye pita mipaka katika upotovu? Je! Unaweza kumfanya asikie aliye kiziwi hasikii la kweli, kipofu hazingatii, na ambaye katika ujuzi wa Mwenyezi Mungu atakufa katika upotovu? Huwezi hayo! Kwa sababu hao wamekwisha thibiti katika ukafiri wao, basi hawanafiki kwa wanayo yasikia, wala wanayo yaona.

41 Basi tukikushika tukakufisha kabla hatuja kuonyesha adhabu yao, na kifua chako kikatua kwa hayo, na pia vifua vya Waumini, alaa kulli hali, Sisi bila ya shaka tutawaadhibu duniani na Akhera.

42 Au unataka tukuonyeshe adhabu tuliyo waahidi kabla ya kufa kwako, tutakuonyesha, kwani Sisi tunawaweza hao kwa uweza wetu na nguvu zetu.

43 Ikiwa moja ya mawili haya lazima liwe bila ya shaka, basi shikamana na Qur'ani tuliyo kufunulia, na simama imara katika kuitekeleza, kwani hakika wewe uko katika Njia ya Haki Iliyo Nyooka.

44 Na hakika hii Qur'ani ni utukufu mkubwa juu yako, ewe Muhammad, na wa Umma wako, kwa kuwa umeteremshiwa kwa lugha ya Kiarabu, na mtakuja kuhojiwa Siku ya Kiyama juu ya haki yake, na shukrani za neema zake.

45 Na hebu angalia katika sharia za Mitume wetu tulio watuma kabla yako. Ati umekuja humo wito wa kuwaita watu wende kuabudu vitu visio kuwa Mwenyezi Mungu? Haukuja! Basi hao wanao abudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu mmoja hadi wamepita mipaka katika upotovu wao!

46. Na bila ya shaka tulimtuma Musa kwa Ishara zetu ende kwa Firauni na waheshimiwa wake, na akasema: Hakika mimi ni Mtume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote!⁴⁶
47. Lakini alipo wajia na Ishara zetu wakaingia kuzicheka.⁴⁷
48. Na hatukuwaonyesha Ishara yoyote ila hiyo ilikuwa kubwa zaidi kuliko nyenginewe. Na tukawakamata kwa adhabu ili warejee.⁴⁸
49. Na wakasema: Ewe mchawi! Tuombe kwa Mola wako Mlezi kwa ile ahadi aliyo kuahidi; hakika sisi tutakuwa wenye kuongoka.⁴⁹
50. Basi tulipo waondolea adhabu hiyo, mara wakaingia kuvunja ahadi.⁵⁰
51. Na Firauni alitangaza kwa watu wake, akisema: Enyi watu wangu! Kwani mimi sinao huu ufalme wa Misri, na hii mito inapita chini yangu? Je! Hamwoni?⁵¹
52. Au mimi si bora kuliko huyu aliye mnyonge, wala hawezi kusema waziwazi?⁵²
53. Basi mbona hakuvikwa vikuku vya dhahabu, au hawakuja Malaika pamoja naye wakamwandama?⁵³
54. Basi aliwachezea watu wake, na wakamt'ii. Kwa hakika hao walikuwa watu wapotovu.⁵⁴
55. Walipo tukasirisha tuliwapatiliza tukawazamisha wote!⁵⁵
56. Kisha tukawafanya kuwa watangulizi na mfano kwa wa baadaye.⁵⁶
57. Na alipo pigiwa mfano Mwana wa Mariamu, watu wako waliupiga ukelele.⁵⁷

46 Na bila ya shaka Sisi tulimtuma Musa tukampa miujiza yenye kuthibitisha ukweli wake, ende kwa Firauni na watu wake. Akasema: Hakika mimi ni Mtume wa Muumba wa walimwengu wote na Mlezi wao nimetumwa kwenu. Wakamtaka aonyeshe miujiza.

47 Alipo wajia kwa miujiza ya kuthibitisha Utume wake mara wakampokea kwa kumcheka, na kumfanyia tashiti, na kumcheza shere, bila ya kuzingatia maneno yake.

48 Na kila muujiza katika miujiza iliyo wajia mfululizo, kwa uwazi wa hoja zake juu ya ukweli wa Mtume, na kuwa kila mmoja peke yake unatimiza makusudio hayo kwa ukamilifu wa kila njia, na ukamilifu wa nafsi yake, hata ukiungalia waweza kusema: Muujiza huu ni mkubwa kuliko ule mwengine. Na walipo shikilia kuendelea na uasi tuliwapatiliza kwa balaa za namna kwa namna, ili warejee, waache upotovu wao.

49 Wakasema, kumlilia Musa balaa zilipo waenea: Ewe mchawi - ndio Mwanachuoni kikwao - Tuombe kwa Mola wako Mlezi, kwa kutawasali na ahadi yake aliyo kupa, atuondolee adhabu hii! Hakika sisi tukifarijiwa bila ya shaka tutaongoka.

50 Mwenyezi Mungu alipo waondolea masaibu yale kwa kuitikia dua za Musa, wakamshitukia kwa kuvunja ile ahadi yao ya kumin.

51 Firauni akawatangazia watu wake kutangaza nguvu zake na madaraka yake: Kwani huu ufalme wa Misri si wangu mimi peke yangu, wala hapana mwenginewe, na hii mito ambayo mnaiona inapita chini ya jumba langu? Hamyaoni haya? Basi hamzingatii mnayo yaona ya nguvu zangu na udhaifu wa Musa? Na Firauni alitaka kwa wito wake kuutia imara ut'ifu wao.

52 Firauni akasema akizidisha ujabari: Bali mimi ni bora kuliko dhaifu huyu mnyonge, asiye weza hata kubainisha wazi huo wito wake kwa ulimi wa fasaha.

53 Akazidi kusema kuchochea kumkadhibisha Musa: Lau ingeli kuwa Mola wake Mlezi angeli mvika vikuku vya dhahabu kwa kumpa funguo za utawala, au akamsaidia kwa Malaika wa kumuunga mkono, ingeli kuwa yeye ni mkweli katika madai yake ya Utume?

54 Firauni akawa anawachochea watu wake, na akawaathiri kwa udanganyifu huu, nao wakamt'ii katika upotovu wake. Kwani hao walikuwa watu walio kwisha toka kwenye Dini ya Mwenyezi Mungu Iliyo Nyooka.

55 Basi walipo tughadhibisha hadi ya kutughadhibisha, kwa kupita kwao mipaka ya ufasaha, tuliwaangamiza kwa kuwazamisha wote.

56 Tukamfanya Firauni na kaumu yake kuwa ni viongozi wa makafiri wa baada yao katika kustahiki mfano wa adhabu yao, na kuwa ni masimulizi ya namna ya ajabu ya watu wote kuyazingatia.

57 Na alipo pigiwa mfano Isa bin Maryam katika kuwa kwake kama Adam kwa kuwa Mwenyezi Mungu

- 58.** Wakasema: Miungu yetu kwani si bora kuliko huyu? Hawakukupigia mfano huo ila kwa ubishi tu. Bali hao ni watu wagomvi!⁵⁸
- 59.** Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa tuliye mneemesha na tukamfanya ni mfano kwa Wana wa Israili.⁵⁹
- 60.** Na tungeli penda tungeli wafanyia miongoni mwenu Malaika katika ardhi wakifuatana.⁶⁰
- 61.** Na kwa hakika yeye ni alama ya Saa ya Kiyama. Basi usiitilie shaka, na nifuateni. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka.⁶¹
- 62.** Wala asikuzuilieni Shet'ani. Hakika yeye ni adui yenu wa dhaahiri.⁶²
- 63.** Na alipo kuja Isa na dalili zilizo wazi, alisema: Nimekujieni na hikima, na ili nikuelezeni baadhi ya yale mliyo khitalifiana. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, na mnit'ii mimi.⁶³
- 64.** Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi, na ni Mola wenu Mlezi. Basi Muabuduni Yeye tu. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka.⁶⁴
- 65.** Lakini makundi kwa makundi yao yalikhitalifiana wao kwa wao. Ole wao walio dhulumu kwa adhabu ya siku chungu.⁶⁵
- 66.** Je! Nini wanangojea ila Saa iwajie kwa ghafla na wala wao hawatambui?⁶⁶
- 67.** Siku hiyo marafiki watakuwa ni maadui, wao kwa wao, isipo kuwa wachamngu.⁶⁷

alimuumba kwa udongo, kisha akamwambia: Kuwa, na akawa. Basi yeye ni mtumwa aliye umbwa, aliye neemeshwa kwa kupewa Unabii, s.l. Haifai kumuabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Na watu wako wanapuza hizo sifa zinazo pigiwa mfano, na wala hawafahamu.

58 Makafiri wamesema: Je! Miungu yetu na Isa, nani bora? Ikiwa yeye yuko Motoni basi sisi na miungu yetu tutakuwa pamoja naye. Hawakupigii mfano huu wewe ila kutafuta ubishi tu, na kushindana kwa maneno, si kwa ajili ya kuitafuta kweli ilivyo. Bali hawa ni watu ambao ni shadidi wa khasama, wamebobeza kwa hayo.

59 Isa si chochote ila ni mja tuliye mneemesha kwa kumpa Unabii, na tumemfanya awe ni zingatiao la ajabu kama ni mithali, kwa kumuumba bila ya baba, kwa Wana wa Israili, wapate ushahidi wa ukamilifu wa uweza wetu.

60 Na lau tungeli taka, tungeli wageza baadhi yenu, enyi watu, mkawa ni Malaika mkifuatana katika ardhi, kama wanavyo kufuateni watoto wenu, mjue kwamba Malaika wananyenyekea kufuata kudra ya Mwenyezi Mungu. Basi vipi wao wastahiki Ungu?

61 Na hakika Isa kwa kuzuka kwake bila ya baba, na kuponyesha kwake vipofu na wakoma ni dalili ya kukaribia Saa ya Kiyama. Basi usiwe na shaka nayo. Na fuateni uwongofu wangu na Mtume wangu. Hii ninayo kuitieni ndiyo Njia Iliyo Nyooka yenye kufikilia Uwokovu.

62 Wala asikuzuilieni Shetani kuifuata Njia Iliyo Nyooka. Hakika huyo ni adui aliye dhaahiri uadui wake.

63 Na alipo tumwa Isa kwa Wana wa Israili naye ana miujiza iliyo wazi, na Ishara zenye kubainisha, aliwaambia: Nimekujieni na sharia yenye hikima nzuri, inayo kuiteni muifuate Tawhidi (Imani ya Mwenyezi Mungu Mmoja). Na nimekujieni nikubainishieni baadhi ya mambo mnayo khitalifiana kwayo katika mambo ya Dini ili mpatane kwenye Haki. Basi iogopeni adhabu ya Mwenyezi Mungu, na mnit'ii mimi katika hayo ninayo kuitieni.

64 Hakika Mwenyezi Mungu, peke yake, ndiye Muumba wangu, na ni Muumba wenu, basi muabuduni Yeye pasi mwengewe. Na ihafidhini sharia yake. Hii ninayo kuitieni muifuate ni Njia Iliyo Nyooka itakayo kufikisheni kwenye uwokovu.

65 Makundi mbali mbali yakakhitalifiana baina ya Wakristo baada ya Isa, kwa kufarikiana juu yake. Maangamizo yatawafika hao walio dhulumu kwa waliyo yasema juu ya Isa ya ukafiri, watapata adhabu kali na chungu Siku ya Kiyama.

66 Makafiri hawangojei kitu baada ya kuipuuza Imani ila kuwafikia Saa kwa ghafla, nao wameghafilika nayo.

67 Marafiki walio kusanyika duniani kwa upotovu, watakuwa maadui wao kwa wao siku itakapo wafikia Saa kwa ghafla, na yatakatika mapenzi yote, ila mapenzi ya wenye kuogopa, nao wangali duniani,

68. Enyi waja wangu! Hamtakuwa na khofu siku hiyo, wala hamtahuzunika.⁶⁸
69. Ambao waliziamini Ishara zangu na walikuwa Waislamu.⁶⁹
70. Ingieni Peponi, nyinyi na wake zenu; mtafurahishwa humo.⁷⁰
71. Watakuwa wanapitishiwa sahani za dhahabu na vikombe; na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanavifurahia, na nyinyi mtakaa humo milele.⁷¹
72. Na hiyo ni Pepo mliyo rithishwa kwa hayo mliyo kuwa mkiyafanya.⁷²
73. Mnayo humo matunda mengi mtakayo yala.⁷³
74. Kwa hakika wakosefu watakaa katika adhabu ya Jahannamu milele.⁷⁴
75. Hawatapumzishwa nayo na humo watakata tamaa.⁷⁵
76. Wala Sisi hatukuwadhulumu, bali wao ndio walio kuwa madhaalimu.⁷⁶
77. Nao watapiga kelele waseme: Ewe Malik! Na atufishe Mola wako Mlezi! Naye aseme: Hakika nyinyi mtakaa humo humo!⁷⁷
78. Kwa yakini tulikuleteni Haki, lakini wengi katika nyinyi mlikuwa mnaichukia Haki.⁷⁸
79. Au waliweza kupitisha amri yao? Bali ni Sisi ndio tunao pitisha.⁷⁹
80. Au wanadhani kwamba hatusikii siri zao na minong'ono yao? Wapi! Na wajumbe wetu wapo karibu nao, wanayaandika.⁸⁰
81. Sema: Ingeli kuwa Rahmani ana mwana, basi mimi ningeli kuwa wa kwanza kumuabudu.⁸¹

kuiogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu, na wakashikamana huko duniani katika kumt'ii Yeye.

68 Mwenyezi Mungu atawaambia wachamngu kwa kuwafanyia hishima: Enyi waja wangu! Leo msikhofu adhabu yoyote, wala msihuzunike. Mmekwisha salimika na adhabu. Na Mwenyezi Mungu amekudhaminieni thawabu.

69 Walio ziamini Ishara za Mwenyezi Mungu na wakamt'ii Yeye, na wakawa wanamnyenyekea.

70 Siku ya Kiyama wataambiwa kwa kufanyiwa hishima: Ingieni Peponi, nyinyi na wake zenu, nanyi mmo katika furaha iliyo kubwa, ambayo itadhihiri kwenye nyuso zenu.

71 . Na baada ya kuingia Peponi watakuwa wakizungukiwa kwa sahani za dhahabu, na bilauri kadhaalika, na humo watapata vyakula namna mbali mbali, na vinywaji vya kila namna. Na humo Peponi watapata kila kitamaniacho moyo, na kituzacho macho. Na kukamilisha furaha wataambiwa: Nyinyi mtakaa milele katika neema hizi.

72 Na kutimiza neema, wataambiwa: Hii ndiyo Pepo mliyo ipata kwa sababu ya vitendo vyema mlivyo vitanguliza mlipo kuwa duniani.

73 Humo mtapata matunda ya namna nyingi, na kwa wingi, mtastarehe kuyala.

74 Hakika walio tenda makosa kwa ukafiri watakuwamo katika adhabu ya Jahannamu daima dawamu.

75 Hawapunguziwi adhabu wakosefu hawa, wala haisitishwi, na wao watakata tamaa ya kuokoka.

76 Wala Sisi hatukuwadhulumu wakosefu hawa kwa adhabu hii, lakini wao wenyewe ndio walio jidhulumu nafsi zao kwa kukhiari upotofu kuliko uwongofu.

77 Na wakosefu, watapo kwisha kata tamaa ya kupunguziwa adhabu kali, watamwita Malik, huyo ni askari wa Motoni wakimwambia: Mwombe Mola wako Mlezi atufishe tupumzike na adhabu ya Jahannamu. Na Malik awambie: Nyinyi mtakaa humu humu katika adhabu milele!

78 Mwenyezi Mungu Mtukufu atawaambia kwa kuwarudi: Nyinyi alikujilieni Mtume wetu, enyi watu wa Makka, kukuleteni Dini ya Haki. Wakaamini wachache, na wengi wenu mkakataa. Nao hawaiipendi Haki.

79 Kwani ndio waliweza washirikina wa Makka kutimiza hivyo vituko vyao kumkadhibisha Mtume na kupanga njama za kumuua? Bali Sisi kwa hakika tuliweza jambo katika kuwalipizia wao na kukupa ushindi wewe juu yao.

80 Ati wanadhani hawa washirikina kwamba Sisi hatuyasikii maneno yao wenyewe wanapo panga njama, na wanapo semezana kwa siri katika kukanusha haki? Kwani! Twawasikia. Na Malaika wanao dhibiti kauli zao wanayaandika hayo.

81 Waambie hao washirikina: Ikihithitika kwa ushahidi kuwa kweli Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema

- 82.** Ametakasika Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, Mola Mlezi wa A'rshi, na hayo wanayo msifa.⁸²
- 83.** Basi waache wapige porojo wakicheza mpaka wakutwe na hiyo siku yao waliyo ahidiwa.⁸³
- 84.** Na Yeye ndiye Mungu mbinguni, na ndiye Mungu katika ardhi. Naye ndiye Mwenye hikima, Mwenye ujuzi.⁸⁴
- 85.** Na ametukuka Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na viliomo ndani yake. Na uko kwake ujuzi wa Saa ya Kiyama, na kwake Yeye mtarudishwa.⁸⁵
- 86.** Wala hao mnao waomba badala yake Yeye hawana uweza wa kumwomba mtu, isipo kuwa anaye shuhudia kwa haki, na wao wanajua.⁸⁶
- 87.** Na ukiwauliza ni nani aliye waumba? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu! Basi ni wapi wanako geuziwa?⁸⁷
- 88.** Na usemi wake (Mtume) ni: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hawa ni watu wasio amini.⁸⁸
- 89.** Basi wasamehe, na uwambie maneno ya salama. Watakuja jua.⁸⁹

ana mwana, basi mimi ningeli kuwa wa kwanza kumuabudu mwana huyo. Lakini hayo hayakuthibiti kwa hoja yoyote kwamba Rahmani ana mwana, kwa kuwa hayo ni kumfanya Mwenye nguvu awe hajiwezi, Mwenye kujitosha awe mhitaji. Na Yeye, *Subhanahu*, ametakasika na kila la upungufu kwa ukamilifu wake.

82 Ametakasika kwa mtakasiko wa Mwenye kuziumba mbingu na ardhi na A'rshi Tukufu, kwa yote wanayo msifa washirikina, ambayo hayaelekeani na Uungu wake.

83 Basi waachilie wazame katika upotovu wao, na wacheze katika dunia yao, wayaache mambo yenye maana, wala wasiyashughulikie, mpaka iwajie Siku ya Kiyama waliyo ahidiwa, ipate kila nafsi kulipwa kwa iliyo yachuma.

84 Na Yeye ndiye anaye abudiwa mbinguni kwa haki, na anaabudiwa katika ardhi kwa haki. Na Yeye, peke yake, ndiye Mwenye hikima za mwisho katika vitendo vyake na mipango yake, Mwenye kujua kila kitu kilicho kuwa na kitakacho kuwa.

85 Na ametukuka na ametaadhamu Yeye ambaye, peke yake, Mwenye ukamilifu wa kutekeleza katika mbingu na ardhi na baina yao katika viumbe vya angani vinavyo onekana na vyenginevyo, na mipango yote iko kwake, na Yeye tu ndiye Mwenye kujua wakati wa Kiyama, na kwake Yeye peke yake, mtarejeshwa mwisho kwa ajili ya hisabu.

86 Na hio miungu yao wanayo iabudu badala ya Mwenyezi Mungu haimiliki uweza wa kuwaomba hao wanao waabudu. Lakini wenye kushuhudia kwa Tawhidi, yaani hao wanao amini ya kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Mola wao Mlezi kwa haki, hao wanaweza kuombewa miongoni mwa Waumini atakao Mwenyezi Mungu kuwaomba.

87 Na ewe Mtume! Ukiwauliza hawa washirikina nani aliye waumba, bila ya shaka watasema: Kawaumba Mwenyezi Mungu. Basi inakuwaje wakaacha kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu wakenda kuwaabudu wengine, nao wanakiri kuwa Yeye ndiye Muumba wao? Ama hakika jambo hili ni la ajabu!

88 Naapa kwa kauli ya Muhammad s.a.w. anapo omba na kuita: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hawa wenye inda ni watu wasio tarajiwa kuamin.

89 Basi waachilie mbali, ewe Mtume, kwa wingi wa inda yao, na waambie: Langu mimi nikukuacheni kwa salama yenu kutoka kwangu, na salama yangu kutoka kwenu. Nanyi mtakuja jua kuwa mwisho wa inda yao ni khasara iliyo wazi.

Sura 44 - Addukhan

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kusimulia khabari za Qur'ani, ya kwamba imeteremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika usiku wa *Lailatul Qadri* ulio barikiwa, kwa ajili ya kuonya na Tawhid, Imani ya Mwenyezi Mungu Mmoja. Na kwamba hii Qur'ani ni Haki, Kweli tupu. Hali kadhaalika Sura imesimulia khabari za kufufuliwa, na kwamba hayo hayana shaka ndani yake, na imezibisha hoja za wanao yakanya hayo, na ikawarudi washirikina. Ikalinganisha baina ya washirikina wa Makka na wenzao walio watangulia, nao ni kaumu ya Firauni. Ikaeleza mapatilizo ya Mwenyezi Mungu yaliyo washukia hao. Tena ikatilia mkazo kwamba Siku ya Kiyama ndiyo siku iliyo pangwa ya kuutenga ukafiri na upotovu wote. Na ikasimulia malipo ya wakosefu kwa siku hiyo na malipo ya walio ongoka. Na ikamalizika kama ilivyo anzia kwa mazungumzo juu ya Qur'ani, na kwa kuwaonya wanao kadhibisha Ujumbe wa Mtume s.a.w. kuwa nao wangojee balaa na masaibu yatakayo washukia.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. H'a Mim¹
2. Naapa kwa Kitabu kinacho bainisha,²
3. Hakika tumekiteremsha katika usiku ulio barikiwa. Hakika Sisi ni Waonyaji.³
4. Katika usiku huu hubainishwa kila jambo la hikima,⁴
5. Jambo litokalo kwetu. Hakika Sisi ndio wenye kutuma.⁵
6. Ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.⁶
7. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilio baina yao, ikiwa nyinyi mna yakini.⁷
8. Hakuna mungu ila Yeye; anahuisha na anafisha- Mola Mlezi wenu na Mola Mlezi wa baba zenu wa mwanzo.⁸

1 H'a Mim. Imeanzia Sura hii kwa baadhi ya harufi za kutamkwa kama ilivyo ada ya Qur'ani katika kufungulia Sura nyingi kwa harufi kama hizi.

2 Mwenyezi Mungu anaapa kwa Qur'ani yenye kuweka wazi Dini ya Haki, yenye kuwabainishia watu yaliyo na maslaaha ya dunia yao na Akhera yao, ili kujulisha utukufu wa cheo chake.

3 Hakika Sisi tumeanza kuteremsha Qur'ani katika usiku ulio jaa kheri, wenye baraka nyingi, kwani ni mwendo wetu kuonya kwa kuwatuma Mitume na kuteremsha Vitabu.

4 Katika usiku huu wenye baraka hupambanuliwa baina ya mambo yote yenye hikima, na Qur'ani ndio kilele cha hikima, na ndio pambanuo baina ya kweli na uwongo. Na kwa hivyo ndio ikateremshwa katika usiku huo.

5 Nakusudia kwa jambo hili, yaani jambo kuu lenye kutoka kwetu kama ilivyo kwisha pita hukumu ya mpango wetu. Kwani ni shani yetu kutuma Mitume kwa Vitabu ili kuwafikishia waja wetu.

6 Kwa ajili ya rehema ya Mola wako Mlezi kwa waja wake, amewatuma Mitume kwa watu wawafikishie uwongofu wake, kwani hakika Yeye peke yake, ndiye Mwenye kusikia kila cha kusikiwa, Mwenye kujua kila cha kujulikana.

7 Yeye ndiye Muumba mbingu na ardhi na vilio baina yao, ikiwa nyinyi mna yakini na haki, na mnaifuata, na mnaamini kuwa hakika ndio Yeye Mwenye kuteremsha Qur'ani kuwa ni rehema na uwongofu.

8 Hapana Mungu isipo kuwa Yeye anaye stahiki kuabudiwa, Yeye peke yake, Mwenye kuhuisha na

9. Lakini wao wanacheza katika shaka.⁹
10. Basi ingoje siku ambayo mbingu zitakapo leta moshi ulio dhaahiri,¹⁰
11. Utakao wafunika watu: Hii ni adhabu chungu!¹¹
12. Mola wetu Mlezi! Tuondolee adhabu hii. Hakika tutaamini.¹²
13. Nini faida ya kukumbuka kwao? Na alikwisha wafikia Mtume mwenye kubainisha.¹³
14. Na wao wakamgeuzia uso, na wakasema: Huyu amefunzwa, naye ni mwendawazimu.¹⁴
15. Hakika sisi tutaiondoa adhabu kidogo, lakini nyinyi kwa yakini mtarejea vile vile!¹⁵
16. Siku tutayo yashambulia mashambulio makubwa, bila ya shaka Sisi ni wenye kutesa.¹⁶
17. Na hakika kabla ya hawa tuliwafanyia mtihani watu wa Firauni, na aliwafikia Mtume Mtukufu.¹⁷
18. Akasema: Nipeni waja wa Mwenyezi Mungu; kwa hakika mimi kwenu ni Mtume Muaminifu.¹⁸
19. Na msimfanyie kiburi Mwenyezi Mungu; hakika mimi nitakuleteeni uthibitisho ulio wazi.¹⁹
20. Nami najikinga kwa Mola wangu Mlezi na ndiye Mola wenu Mlezi pia, ili msinipige mawe.²⁰
21. Na ikiwa hamniamini, basi jitengeni nami.²¹

kufisha. Na Yeye peke yake, ndiye aliye kuumbeni nyinyi na kawaumba baba zenu wa mwanzo.

9 Lakini makafiri wana shaka na ukweli huu, wamo wakifuata pumbao lao. Na huo ndio mtindo wa watu wa pumbao na michezo, sio mwendo wa watu wa ilimu na yakini.

10 Basi ewe Mtume! Ngojea ukame utapo wateremkia, wakasibiwa na kukonda na udhaifu wa kuona, ikawa mtu huwa anaona baina ya mbingu na ardhi moshi dhaahiri shaahiri, akawa anasikia mvumo wake wala hauoni.

11 Moshi huu utawazunguka wale wanao kadhibisha walio sibiwa na ukame, watasema kwa wingi wa kitisho: Hii ni adhabu kali na chungu!

12 Kama pia watavyo sema kwa kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu: Hakika sisi tutaamini ukituondolea adhabu ya njaa na dhiki.

13 Watu hawa watawaidhika vipi, hata watimize hiyo Imani wanayo iahidi wakiondolewa adhabu, na hali Mtume mwenye ujumbe ulio wazi keshwa wajia na miujiza yenye kuonyesha ukweli wake, na hayo ndiyo mawaidha makubwa kabisa?

14 Kisha wakaacha kumsadiki Mtume aliye tiliwa nguvu na miujiza iliyo wazi, na wakamwambia: Huo uwongo na uzushi! Mara nyengine wakimsingizia kuwa amefunzwa hayo na mtu, na mara nyengine kuwa akili yake imekorogeka.

15 Mwenyezi Mungu anawarudi: Sisi hakika tutakuondoleeni adhabu wakati wa duniani, nao ni wakati mchache, lakini nyinyi mtarejea tu, bila ya shaka, yale yale mliyo kuwa mkiyatenda.

16 Ewe Mtume! Watajije ile siku tutapo washika kwa mshiko mkubwa, wa nguvu. Nasi kwa mshiko huu ndio tunawatesa.

17 Na bila ya shaka tulikwisha wafanyia mtihani, kabla ya makafiri wa Makka, kaumu ya Firauni kwa kuwaitia kwenye Imani, na akawajia Musa, Mtume Mtukufu kwa Mwenyezi Mungu. Wakamkataa kwa inda tu. Na huo ndio mtindo wa hawa washirikina.

18 Mtume Mtukufu aliwaambia: Nipeni enyi waja wa Mwenyezi Mungu lilio waajibu juu yenu, nalo ni kuitikia wito wangu, kwani mimi ni Mtume nimetumwa makhsusi kwenu, na ni muaminifu katika ujumbe wangu.

19 Wala msimfanyie kiburi Mwenyezi Mungu kwa kumkadhibisha Mtume wake, kwani mimi nakuleteeni muujiza ulio wazi wa kubainisha ukweli wa Unabii wangu na Utume wangu.

20 Na mimi najilinda na Mwenye kuniumba msiweze kuniuwa kwa kunipiga mawe.

21 Na ikiwa hamnisadiki basi jitengeni nami, wala msiniudhi.

22. Ndipo akamwomba Mola wake Mlezi: Hakika watu hawa ni wakosefu.²²
23. Mwenyezi Mungu akasema: Basi nenda na waja wangu usiku. Kwa yakini mtafuatwa.²³
24. Na iache bahari vivyo hivyo imeachana, hakika wao hao ni jeshi litakalo zamishwa.²⁴
25. Mabustani mangapi, na chemchem ngapi waliziacha!²⁵
26. Na mimea na vyeo vitukufu!²⁶
27. Na neema walizo kuwa wakijistareheshea!²⁷
28. Ndio hivyo! Na tukawarithisha haya watu wengine.²⁸
29. La mbingu wala ardhi hazikuwalilia, wala hawakupewa muhula.²⁹
30. Na bila ya shaka tuliwaokoa Wana wa Israili katika adhabu ya kuwadhalilisha,³⁰
31. Ya Firauni. Hakika yeye alikuwa jeuri katika wenye kupindukia mipaka.³¹
32. Na tuliwakhiari kwa ujuzi wetu kuliko walimwengu wengine.³²
33. Na tukawapa katika ishara zenye majaribio yaliyo wazi.³³
34. Hakika hawa wanasema:³⁴
35. Hapana ila kufa kwetu mara ya kwanza tu, wala sisi hatufufuliwi.³⁵
36. Basi warudisheni baba zetu, ikiwa nyinyi mnasema kweli.³⁶
37. Je! Ni wao bora au watu wa Tubbaa' na walio kuwa kabla yao? Tuliwaangamiza. Hakika hao walikuwa wakosefu.³⁷

22 Musa akamwambia Mola wake Mlezi kwa kumshitakia watu wake alipo kata tamaa nao kuwa hawaamini: Hakika watu hawa shauri yao imekwisha fika ukomo katika ukafiri; basi Wewe wafanyie wanalo stahiki.

23 (Naye Musa akaambiwa:) Toka na Waumini usiku usiku kwa kificho, wasije kukupateni, kwani Firauni na askari wake watakuafuteni pindi wakijua, wakukamateni.

24 Na iache bahari imetulia kama ilivyo baada ya kwisha pigwa kwa fimbo, wapate kuingia hao wanao kanya; kwani wao watazama tu, hapana hivi wala hivi.

25 Hao watu wa Firauni baada ya kuzama kwao waliacha mabustani mengi yenye kunawiri, na chemchem zinazo tiririka maji yake,

26 Na makulima ya namna kwa namna, na makaazi mazuri mazuri,

27 Na maisha ya raha na starehe, waliyo kuwa wakiyaonea utamu.

28 Mfano wa adhabu hiyo Mwenyezi Mungu humuadhibu mwenye kwenda kinyume na amri yake, na akatoka katika ut'iifu wake, na humwondolea neema yule mwenye nayo akawapa watu wengine wasio kuwa na makhusiano nao yoyote, la ya ujamaa wala dini.

29 Basi la mbingu wala ardhi hazikuwahuzunukia ilipo wanyakua adhabu, jinsi ilivyo haribika hali yao; wala hawakungojewa watubu, wala hawakupewa muhula wapate kudiriki taksiri yao, kwa jinsi walivyo dharauliwa!

30 Na kwa hakika Mwenyezi Mungu aliwaokoa Wana wa Israili na adhabu ya kuwadhalilisha.

31 . Aliwaokoa kwa Firauni. Hakika Firauni alikuwa jeuri kwa watu wake, amepita mipaka kwa shari na uasi.

32 Ninaapa: Tuliwakhiari Wana wa Israili kwa kuwa tuliwajua kwamba wao wana stahiki kuteuliwa kuliko watu wengine wote wa zama zao. Kwa hivyo tukawatuma miongoni mwao Manabii wengi kwa kuwa tulijua hali zao.

33 Na Mwenyezi Mungu akawaletela katika mkono wa Musa dalili kadhaa wa kadhaa za kuwatia wao katika mitihani iliyo wazi.

34 Hakika hawa wanao kadhibisha kufufuliwa bila ya shaka wanasema: Hapana kufa ila kwa haya haya mauti yetu ya kwanza ya duniani, wala sisi hatutafufuliwa tena.

35 Tazama tanbihi ya 34.

36 Na wao humwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu na Waumini: Ikiwa nyinyi mnasema kweli katika madai yenu kwamba Mola wenu Mlezi anahusha wafu kwa ajili ya hisabu katika Akhera, basi upesi upesi tufufulieni baba zetu walio kwisha kufa, kwa kumwomba huyo Mola wenu Mlezi!

37 Je! Makafiri wa Makka wanawashinda kaumu ya Tubbaa' na walio watangulia kwa nguvu, na

38. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo.³⁸
39. Hatukuviumba hivyo ila kwa Haki, lakini wengi wao hawajui.³⁹
40. Hakika siku ya Uamuzi ni wakati ulio wekwa kwa wao wote.⁴⁰
41. Siku ambayo rafiki hatamfaa rafiki yake kwa chochote, wala hawatanusuriwa.⁴¹
42. Isipo kuwa atakaye mrehemu Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye kurehemu.⁴²
43. Hakika Mti wa Zaqqum,⁴³
44. Ni chakula cha mwenye dhambi.⁴⁴
45. Kama shaba iliyo yayushwa, hutokota matumboni⁴⁵
46. Kama kutokota kwa maji ya moto.⁴⁶
47. (Itasemwa:) Mkamateni na mtupeni katikati ya Jahannamu!⁴⁷
48. Kisha mmwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji yanayo chemka.⁴⁸
49. Onja! Ati wewe ndiye mwenye nguvu, mtukufu!⁴⁹
50. Hakika haya ndiyo mliyo kuwa mkiyatilia shaka.⁵⁰
51. Hakika wachamngu watakuwa katika mahali pa amani,⁵¹
52. Katika mabustani na chemchem,⁵²
53. Watavaa hariri nyepesi na hariri nzito wakikabiliana,⁵³

ulinzi, na utawala, na mambo yote ya kidunia? Ewe Muhammad! Hao washirikina wa kaumu yako hawawashindi hao kwa nguvu, na hao Sisi tuliwateketeza katika dunia kwa ukafiri wao na madhambi yao. Basi nawawazingatie!

38 Na Mwenyezi Mungu hakuumba mbingu na ardhi na viliomo baina yao bila ya hikima

39 Hatukuziumba hizo ila kwa umbo lililo ambatana na hikima, kwa nidhamu iliyo thibiti yenye kuonyesha ushahidi wa kuwepo Mwenyezi Mungu wa pekee, Mwenye uwezo. Lakini wengi wa hawa wameghafilika, wamo katika upofu, hawazioni dalili hizi.

40 Hakika siku ya hukumu kupambanua baina ya mwenye haki na asiye na haki, ni wakati walio ahidiwa wote.

41 Siku ambayo jamaa hawezi kumtetea jamaa yake, wala rafiki kumtetea rafiki yake kwa lolote, hata kwa uchache wa adhabu. Wala wao hawatanusuriwa nafsi zao mbele ya Mwenyezi Mungu.

42 Lakini wale ambao Mwenyezi Mungu amewarehemu, miongoni mwa Waumini, Mwenyezi Mungu atawasamehe, na atawapa ruhusa ya uombezi waweze kuwaombea wenginewe. Hakika Yeye ndiye Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye kuwarehemu waja wake Waumini.

43 Hakika mti wa Zaqqumu unao juulikana kwa ubaya wa sura yake, na ukarihi kuula kwake, na harufu yake, ni chakula cha wakosefu weny madhambi mengi.

44 Tazama tanbihi ya 43.

45 Utamu wake kama maadeni iliyo yayushwa kwa moto, inatokota matumboni kama yanavyo tokota maji yanayo chemshwa.

46 Tazama tanbihi ya 45.

47 Enyi Mazabania wa Jahannamu (Walinzi wa Motoni)! Mkamateni huyu mkosefu, mwenye dhambi, mumtokomezwa kwa nguvu na ukali mpaka katikati ya Jahannamu!

48 Kisha mmiminieni juu ya kichwa chake maji ya moto makali kuzidi kumuadhibu na kumtesa.

49 Ataambiwa kwa kejeli na maskhara: Onja hii adhabu kali, kwani ati wewe si ndiye mtukufu mwenye nguvu katika kaumu yako, ndiye mheshimiwa unavyo jiona mwenyewe!

50 Hapana shaka hii adhabu mnayo ipata ni kweli yenye kuwa, na ndiyo mliyo kuwa mkiibisha duniani, na mkiitilia shaka kuwa haiwi.

51 Hakika hao ambao wamejikinga nafsi zao na maasi kwa kufuata ut'iifu wa Mwenyezi Mungu wapo pahala patukufu ambapo ndani yake wao wanajipatia amani kwa nafsi zao.

52 Katika mabustani watapo kuwa ndani yake wanastarehe, na chemchem za maji yanayo pita chini yao, kwa sababu ya kuwakirimu wao kwa kutukuza hizo neema zao.

53 Wakivaa humo hariri nyepesi na nzito kuzidi kuongeza mapambo yao, nao wakielekeana katika majlisi zao, ili kutimiza starehe.

54. Hivi ndivyo itakavyo kuwa, na tutawaoza mahurilaini.⁵⁴
55. Humo watataka kila aina ya matunda, na wakae kwa amani.⁵⁵
56. Humo hawataonja mauti ila mauti yale ya kwanza, na (Mwenyezi Mungu) atawalinda na adhabu ya Jahannamu,⁵⁶
57. Kuwa ni fadhila zitokazo kwa Mola wako Mlezi. Huko ndiko kufuzu kukubwa.⁵⁷
58. Basi tumeifanya nyepesi hii Qur'ani kwa ulimi wako, ili wapate kukumbuka.⁵⁸
59. Ngoja tu, na wao wangoje pia.⁵⁹

54 Na pamoja na malipo haya tutawaoza huko Peponi mahurilaini, ambao huwezi kuwachanganyia jicho kwa hadi ya uzuri wao na ukubwa wa macho yao.

55 Nao huko Peponi watataka kila tunda wanalo litamani, kwa kujua kuwa hayatawaletea vimbizi, wala hayatakwisha, wala hayataadimika.

56 Huko Peponi hawataonja mauti baada ya mauti ya kwanza waliyo kwisha yaonja duniani ulipo kwisha muda wao wa kuishi, na Mola wao Mlezi atawalinda na adhabu ya Motoni.

57 Kuhifadhiwa kwao na adhabu ni fadhila na hisani ya Muumba wako. Kuhifadhiwa huko na adhabu na kuingizwa kwao Peponi ndio hadi ya mwisho ya kufuzu kulio kukubwa.

58 Basi hakika Sisi tumekufanyia wepesi kuisoma Qur'ani na kuifikisha kama ilivyo teremka kwa lugha yako, na lugha yao, ili wapate kuwaidhika, na waiamini, na watende kwa mujibu yaliomo ndani yake.

59 Basi wewe yangojee hayo yatakayo wafika, na wao pia wanangojea yatakayo kufika wewe na huo wito wako, mambo yakibadilika.

Sura 45 - Al-Jaathiya

Utangulizi

Imeanzia Sura hii kwa harufi mbili katika harufi za Alifbete, na ikafuatiliza kwa kubainisha kuwa kuteremshwa Qur'ani kumetokana na Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu Mwenye hikima. Kisha ikazitaja dalili za uumbaji na za kiakili kuthibitisha itikadi ya Imani na kuitia watu waifuata. Hali kadhaalika imekusanya wito kwa wenye kukadhibisha Ishara. Kisha ikaingia kuzihisabu neema za Mwenyezi Mungu na fadhila zake kwa waja wake; na ikawataka Waumini wawasamehe makafiri wanao kanya. Kwani Mwenyezi Mungu peke yake ndiye wa kumlipa kila mtu kwa alilo litenda. Kisha Sura baada ya hayo ikazungumzia vipi Mwenyezi Mungu alivyo wafadhili Wana wa Israili kwa kuwapa neema nyingi, na khitilafu zilizo zuka baina yao ambazo Mwenyezi Mungu atazitolea hukumu Siku ya Kiyama. Kisha ikaingia kufarikisha baina ya walio fuata Haki na walio fuata matamano, wakakanya kufufuliwa, na wakapinga Ishara za uweza kwa kutaka wafufuliwe baba zao! Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuhuisha, na ndiye Mwenye kufisha. Yeye ana ufalme wa kila kitu. Na siku watakapo kusanywa wapotovu kila nafsi itaitwa ikapokee kitabu chake. Hapo watafuzu Waumini na watakemewa walio takabari. Sura tena inarejea hadithi ya kule kuikataa kwao Saa ya Kiyama, na kuzikadhibisha Ishara zinazo ionyesha; na vile Mwenyezi Mungu atavyo wasahau wao kama wao walivyo isahau hii Siku. Na ikabainisha kuwa makaazi yao ni Motoni kwa kule kuzikejeli kwao Ishara za Mwenyezi Mungu na kudanganyika kwao na dunia. Na Sura imekhitimisha kwa kumsifu Muumba mbingu na ardhi, Mwenye utukufu kote humo, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. H'a Mim¹

2. Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.²

3. Hakika katika mbingu na ardhi ziko Ishara kwa Waumini.³

4. Na katika umbo lenu na katika wanyama alio watawanya zimo Ishara kwa watu wenye yakini.⁴

1 H'a Mim. Hizi ni harufi mbili katika harufi za kutamkwa, zimeanzia Sura hii kama ada ya Sura nyingi katika Qur'ani ambazo zimeanzia kwa harufi kama hivi ili kuashiria kuwa washirikina wameshindwa kuleta mfano wake, ijapo kuwa hii Qur'ani imeundwa kwa harufi hizi hizi wanazo zitumia katika maneno yao.

2 Huu mteremsho wa Qur'ani umetokana na Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Asiye shindika, Mwenye hikima katika kupanga kwake na kuendesha kwake.

3 Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi ni katika ufundi wa namna ya pekee wa Mwenyezi Mungu, bila ya shaka ni dalili zenye nguvu kabisa katika Ungu wake na Upweke wake, ambao wanauamini wenye kumsadiki Mwenyezi Mungu kwa maumbile yao yaliyo sawa.

4 Na vile Mwenyezi Mungu kukuumbeni nyinyi, enyi watu, kama mlivyo, mna sura nzuri, na umbo la peke yenu, na mnavyo khitalifiana baina ya wanaadamu na wanyama na mkaenezwa ulimwenguni, na

5. Na kupishana usiku na mchana, na riziki anayo iteremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwayo akaifufua ardhi baada ya kufa kwake, na mabadiliko ya upepo, ni Ishara kwa watu wenye akili.⁵
6. Hizi Aya za Mwenyezi Mungu tunakusomea kwa haki; basi hadithi gani watakayo iamini baada ya Mwenyezi Mungu na Aya zake?⁶
7. Ole wake kila mzushi mwenye dhambi!⁷
8. Anaye sikia Aya za Mwenyezi Mungu akisomewa, kisha anashikilia yale yale aliyo katazwa, na anajivuna, kama kwamba hakuzisikia. Basi mbashirie adhabu chungu!⁸
9. Na anapo kijua kitu kidogo katika Aya zetu hukifanyia mzaha. Watu hao ndio watakao kuwa na adhabu ya kufedhehesha.⁹
10. Na nyuma yao ipo Jahannamu. Na walio yachuma hayatawafaa hata kidogo, wala walinzi walio washika badala ya Mwenyezi Mungu. Na watapata adhabu kubwa.¹⁰
11. Huu ni uwongofu. Na wale wale walio zikataa Ishara za Mola wao Mlezi watapata adhabu inayo tokana na ghadhabu iliyo chungu.¹¹
12. Mwenyezi Mungu ndiye aliye ifanya bahari ikutumikieni, ili humo zipite marikebu kwa amri yake, na ili mtafute fadhila yake, na mpate kushukuru.¹²
13. Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri.¹³

manufaa mbali mbali, bila ya shaka ni Ishara zenye nguvu na ziwazi kwa watu wanao tafuta yakini ya mambo yao kwa kuzingatia na kufikiri.

5 Na katika kukhitalifiana usiku na mchana, kwa urefu na ufupi, na mwangaza na giza, na kupeana zamu kwa nidhamu iliyo thibiti, na katika mvua anayo iteremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, akaihuisha ardhi kwa mimea baada ya kufa kwake kwa ukame, na kuziendesha pepo pande mbali mbali nazo zinakhitalifiana kwa ubaridi na joto, na nguvu na udhaifu, ni alama zilizo wazi za kuonyesha ukamilifu wa uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa watu wenye kufikiri kwa akili zao, wakafikilia yakini yao.

6 Hizo ni Aya za Mwenyezi Mungu zinazo eleza uumbaji alio ufanya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya watu. Tunakusomea wewe katika Qur'ani kwa ulimi wa Jibrili, nazo Aya hizo ni za haki. Ikiwa hao hawaziamini hizi basi maneno gani watayasadiki baada ya maneno ya Mwenyezi Mungu, nayo ni Qur'ani na Aya zake.

7 Atapata maangamizo makubwa kila anaye mzulia Mwenyezi Mungu uwongo mbaya, na mwenye kukithiri madhambi yake kwa kitendo hicho!

8 Mzushi kama huyu husikia Aya za Mwenyezi Mungu akisomewa, nazo zinasema haki tupu. Kisha yeye huendelea na ukafiri wake kwa kutakabari, akaikataa Imani. Hali yake ni hali ya asiye pata kuzisikia Aya. Basi ewe Nabii! Mbashirie, kwa kumkejeli, kuwa atapata adhabu chungu kwa huko kushikilia kwake kitendo kitacho mletea adhabu hiyo.

9 Na huyu mwenye inda, akijua kitu kidogo katika Aya za Mwenyezi Mungu huzifanya Aya zote za Mwenyezi Mungu ni kitu cha kufanyia maskhara na mzaha. Wazushi hao wingi wa madhambi watapata adhabu ya kuwadhalilisha kwa kiburi chao.

10 Nyuma yao ipo Jahannamu inawangojea, na walicho kichuma duniani hakitawapunguzia hata chembe ya adhabu yake. Wala hiyo miungu ya uwongo walio ifanya ndio ya kuwanusuru badala ya Mwenyezi Mungu, haitawakinga na chochote katika adhabu yake. Na wao watapata mateso makubwa, kwa kitisho chake na ukali wake.

11 Hii Qur'ani ni ushahidi kaamili wa Haki itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na hao wanao zikataa hoja zililo kusanywa na Qur'ani zilizo toka kwa Muumba wao na Mlezi wao watapata adhabu kali mno miongoni mwa namna za adhabu.

12 Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye kufanyieni ikutumikieni bahari ili marikebu zipate kwenda juu yake kwa idhini yake, na uwezo wake, zikikubebeni nyinyi na bidhaa zenu, na ili mtafute kutokana na fadhila za Mwenyezi Mungu mali ya baharini kwa kupata manufaa ya ujuzi, na biashara, na jihadi, na zawadi, na uvuvi, na kutoa vyombo, na ili mpate kushukuru neema zake kwa kumsafia Dini Mwenyezi Mungu.

13 Na akakudhalilishieni vyote viliomo mbinguni, nyota zenye kung'ara na sayari, na vyote viliomo

14. Waambie walio amini wawasamehe wale wasio zitaraji siku za Mwenyezi Mungu, ili awalipe kwa waliyo kuwa wakiyachuma.¹⁴
15. Mwenye kutenda mema basi ni kwa ajili ya nafsi yake, na mwenye kutenda uovu ni juu yake mwenyewe. Kisha mtarudishwa kwa Mola wenu Mlezi.¹⁵
16. Na hakika tuliwapa Wana wa Israili Kitabu na hukumu na Unabii, na tukawaruzuku vitu vizuri vizuri, na tukawafadhilisha kuliko walimwengu wote.¹⁶
17. Na tukawapa maelezo wazi ya amri. Basi hawakukhitalifiana ila baada ya kuwajia ujuzi, kwa ajili ya uhasidi uliyo kuwa baina yao. Hakika Mola wako Mlezi atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika mambo waliyo kuwa wakikhitalifiana.¹⁷
18. Kisha tukakuweka wewe juu ya Njia ya haya mambo, basi ifuate, wala usifuate matamano ya wasio jua kitu.¹⁸
19. Kwa hakika hao hawatakufaa kitu mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hakika wenye kudhulumu ni marafiki wao kwa wao. Na Mwenyezi Mungu ni rafiki wa wamchao.¹⁹
20. Hizi ni dalili zilizo wazi kwa watu wote, na ni uwongofu, na rehema kwa watu wanao yakinisha.²⁰
21. Je! Wanadhani wanao tenda maovu kuwa tutawafanya kama walio amini, na wakatenda mema, sawa sawa uhai wao na kufa kwao? Ni hukumu mbaya wanayo ihukumu!²¹
22. Na Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa haki, na ili kila nafsi ilipwe

kwenye ardhi, makulima, mifugo, maji, moto, hewa, na jangwa, vyote hivyo vinatokana na Yeye Mtukufu, ili akuenezeni manufaa ya uhai. Hakika katika hizo neema zilizo tajwa zipo Ishara zenye kuonyesha kudra yake kwa watu wenye kuzingatia Ishara.

14 . Ewe Mtume! Waambie wanao msadiki Mwenyezi Mungu na wanakufuata wewe, wasamehe maudhi yanayo wafikia kutokana na watu ambao hawataraji kuja siku za Mwenyezi Mungu za kuwalipa watu kwa kheri na shari kwa mujibu walivyo.

15 . Mwenye kutenda mema atapata ujira wake na thawabu mwenyewe; na mwenye kutenda uovu basi dhambi za kitendo chake zitamuangukia mwenyewe. Kisha mtarudishwa kwa Muumba wenu kwa ajili ya malipo.

16 Ninaapa kwa hakika tumewapa Wana wa Israili Taurati, na hukumu iliomo ndani yake, na Unabii ulio funuliwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na tumewaruzuku kheri namna mbali mbali, na tumewafadhilisha wao katika neema nyingi juu ya viumbe vyote.

17 Na tumewapa dalili wazi katika mambo ya Dini yao. Basi haikutokea khitalifu baina yao ila baada ya kwisha wajia ujuzi wa hakika ya Dini na hukumu zake. Na hayo ni kwa uadui na uhasidi tu ulio baina yao. Hakika Mola wako Mlezi atapambanua baina ya hao wanao khitalifiana Siku ya Kiyama katika mambo waliyo kuwa wamekhitalifiana.

18 Tena tukakujaalia wewe, ewe Muhammad, baada ya khitalifu za Watu wa Kitabu (yaani Mayahudi na Wakristo), kuwa ni Mtume wa kwenda Njia iliyo wazi katika mambo ya Dini tuliyo kuwekea wewe na walio kuwa kabla yako miongoni mwa Mitume. Basi ifuate Sharia yako ya Haki, yenye kuthibiti imara kwa hoja na dalili, wala usifuate matamano ya watu wasio ijua Njia ya Haki.

19 Hakika hao waongo wenye tamaa ya kuwa ati wewe utawafuata wao, hawatoweza kukuondolea hata chembe ya adhabu pindi ukiwafuata. Na hakika wenye kupindukia mipaka ya Mwenyezi Mungu husaidiana wao kwa wao katika upotovu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuwasaidia wale wanao mcha, basi hao haitawafikia dhulma ya wenye kudhulumu.

20 Hii Qur'ani ulio teremshiwa wewe ni dalili kwa watu kuwaonyesha Dini ya Haki, na uwongofu wa kuwaongoza kwenye njia za kheri, na neema kwa watu wenye kuyakinisha thawabu na adhabu za Mwenyezi Mungu.

21 Bali wanadhani hao walio chuma yanayo chusha katika ukafiri na maasi kwamba tutawafanya kama walio muamini Mwenyezi Mungu na wakatenda vitendo vyema, na hivyo tuwafanye sawa baina ya makundi mawili hayo katika uhai na katika kufa? Hukumu yao ni mbaya mno, ikiwa wanahisi kuwa wao ni sawa na Waumini.

yale iliyo yachuma. Nao hawatadhulumiwa.²²

23. Je! Umemwona aliye fanya matamaniao yake kuwa ndiye mungu wake, na Mwenyezi Mungu akamwacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi, na akapiga muhuri juu ya masikio yake, na moyo wake, na akambandika vitanga machoni mwake? Basi nani atamwongoa huyo baada ya Mwenyezi Mungu? Hamkumbuki?²³

24. Na walisema: Hapana ila huu uhai wetu wa duniani - twafa na twaishi, na hapana kinacho tuhiliki isipo kuwa dahari. Lakini wao hawana ilimu ya hayo, ila wao wanadhani tu.²⁴

25. Na wakisomewa Aya zetu zilizo wazi hawana hoja ila kusema: Waleteni baba zetu, ikiwa nyinyi ni wasemao kweli.²⁵

26. Sema: Mwenyezi Mungu anakuhuisheni, kisha anakufisheni, kisha anakukusanyeni Siku ya Kiyama isiyo na shaka. Lakini watu wengi hawajui.²⁶

27. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Na siku itapo simama Saa ya Kiyama, siku hiyo wataangamia wenye kushikamana na upotovu.²⁷

28. Na utauona kila umma umepiga magoti, na kila umma utaitwa kwenda soma kitabu chake: Leo mtalipwa mliyo kuwa mkiyatenda.²⁸

29. Hichi kitabu chetu kinasema juu yenu kwa haki. Hakika Sisi tulikuwa tukiyaandika mliyo kuwa mkiyatenda.²⁹

30. Ama walio amini na wakatenda mema, Mola wao Mlezi atawatia katika rehema yake. Huko ndiko kufuzu kulio wazi.³⁰

22 Na Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa mujibu wa hikima na nidhamu, ili zidhihiri dalili za Ungu wake na uwezo wake, na apate kulipwa kila mtu kwa alilo tenda, ikiwa kheri au shari. Na wao hawatapunguziwa chochote katika malipo yao.

23 Ewe Mtume! Umeangalia, ukamwona huyo mwenye kufanya matamaniao yake ndiye mungu wake wa kumuabudu, akamnyenyekea, na akamt'ii, na akaiacha Njia ya Haki na hali anaijua, na akaziba masikio yake asisikie waadhi, na moyo wake asiamini Haki, na akabandika vitanga vya macho asione ya kuzingatiwa? Basi nani wa kumwongoa mtu huyu baada ya kwisha puuzwa na Mwenyezi Mungu? Je! Mnaacha kutazama ili msipate kukumbuka?

24 Na walisema wenye kukanya kufufuliwa: Hapana uhai ila huu uhai wa duniani tu tulio nao sasa. Tunaishi na tunakufa. Na hapana nyuma ya hayo uhai baada ya kwisha kufa. Na hapana cha kututeketeza isipo kuwa kupita dahari, yaani zama na wakati. Wala wao hawasemi hayo kwa ujuzi na kuwa na yakini, bali ni kwa kudhania na kukisia tu.

25 Na ukiwasomea Aya za Mwenyezi Mungu zilizo wazi zenye kuonyesha uwezo wake wa kufufua, huwa hawana hoja ila kusema - kwa kuikambia haki: Wafufueni baba zetu, ikiwa nyinyi ni wasema kweli katika kudai kuwa kupo kufufuliwa.

26 Ewe Muhammad! Waambie: Mwenyezi Mungu amekupeni uhai duniani nanyi hamkuwa chochote, kisha anakufisheni unapo timia wakati wenu. Kisha atakukusanyeni Siku ya Kiyama, na hapana shaka ya kukusanywa huko. Lakini wengi wa watu hawajui uwezo wa Mwenyezi Mungu wa kufufua, kwa sababu ya mapuuzwa yao kuzingatia dalili ziliopo. Na huyo Muweza wa hayo pia ni Muweza wa kuwaleta baba zenu.

27 Na ni wa Mwenyezi Mungu pekee ufalme wa mbingu na ardhi, kwa kuumba, kumiliki, na kupanga. Na itapo fika Saa ya Kiyama, siku hiyo watakhasiri wenye kufuata upotovu.

28 Ewe unaye semezwa! Utawaona siku itapo fika Saa watu wa kila dini wamekalia magoti kwa khofu haliyo nayo kungojea kuitikia wito. Kila umma utaitwa kwenye daftari la vitendo vyao, na wataambiwa: Leo mtalipwa sawa malipo ya mliyo kuwa mkiyatenda duniani.

29 Na wataambiwa: Hichi hapa kitabu chetu tulimo sajili vitendo vyenu, nanyi mmekichukua kwa mikono yenu, kinataja juu yenu yale mliyo yatenda kwa ushahidi wa kweli. Hakika Sisi tulikuwa tukiwataka Malaika waandike, ili tupate kukuhasibieni yaliyo tokana nanyi.

30 Basi ama walio amini na wakatenda vitendo vyema, Mola wao Mlezi atawatia katika Pepo yake. Malipo hayo ndio kufuzu kulio bainika, kulio wazi.

31. Na ama walio kufuru, wataambiwa: Kwani hamkuwa mkisomewa Aya zangu nanyi mkapanda kichwa, na mkawa watu wakosefu?³¹
32. Na ikisemwa: Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, na Saa haina shaka, nyinyi mkisema: Hatuijui hiyo Saa, tunadhania dhana tu, wala hatuna yakini.³²
33. Basi ubaya wa waliyo yatenda utawadhahirikia, na yatawazunguka waliyo yafanyia maskhara.³³
34. Na itasemwa: Leo tunakusahauni kama nyinyi mlivyo sahou mkutano wa siku yenu hii; na mahali penu ni Motoni, wala hamna wa kukunusuruni.³⁴
35. Hayo ni kwa sababu nyinyi mlizifanyia mzaha Aya za Mwenyezi Mungu; na maisha ya dunia yakakudanganyeni. Basi leo hawatatolewa humo wala hao hawatakubaliwa udhuru wao.³⁵
36. Basi sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa mbingu, na Mola Mlezi wa ardhi, na Mola Mlezi wa walimwengu wote.³⁶
37. Na ukubwa ni wake Yeye tu, mbinguni na katika ardhi, naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.³⁷

31 Na ama walio mkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake wataambiwa kwa kuwahizi: Kwani hawakukujilieni Mitume wangu? Hamkusomewa Aya zangu, nanyi mkajiona bora hamfai kuikubali haki, na mkawa kaumu ya makafiri?

32 Enyi mnao kanya kufufuliwa! Akikwambieni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwamba agano la Mwenyezi Mungu la kuwalipa ni haki yenye kuthibiti, na Saa haina shaka itakuja, nyinyi mkisema: Sisi hatujui chochote khabari ya hiyo Saa ya Kiyama, wala ukweli wake; na sisi ni dhana ya kudhania tu kuwa hiyo Saa itakuja, wala hatuna yakini kuwa itatokea

33 Na utawadhahirikia hawa makafiri ubaya wa vitendo vyao, na itawatermkia jaza ya maskhara yao waliyo kuwa wakizifanyia Ishara za Mwenyezi Mungu.

34 Na wataambiwa hawa washirikina kwa kuwahizi: Leo hii tunakuacheni katika adhabu kama nyinyi mlivyo acha kujitayarisha kukutana na Mola wenu Mlezi katika siku hii kwa ut'iifu na vitendo vyema. Na pahala penu pa kukaa ni Motoni, na wala hamna wa kukunusuruni akakuokoeni na adhabu yake.

35 Adhabu hiyo imekuteremkieni kwa sababu ya ukafiri wenu, na maskhara yenu kuzifanyia Ishara za Mwenyezi Mungu, na mlivyo khadaika na maisha ya dunia kwa mapambo yake. Basi leo hapana yeyote awezaye kuwatoa hawa kwenye Moto, wala hawatakikani kumtaka radhi Mola wao Mlezi kwa kutafuta udhuru.

36 Basi ni za Mwenyezi Mungu pekee sifa njema, Muumba mbingu na ardhi, na Muumba wa viumbe vyote. Kwani hivi kuwa ni Mola Mlezi wa kila kitu unawajibika uhimidiwe kwa neema zote.

37 Na ni wake Yeye, *Subhanahu*, utukufu na utawala katika mbingu na ardhi. Na Yeye ni Mwenye nguvu, asiye shindika, Mwenye hikima, asiye kosea katika hikima yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi kuliko wote.

Sura 46 - Al-Ah'qaaf

Utangulizi

Sura hii tukufu inasimulia kuteremka kwa Qur'ani kutokana na Mwenyezi Mungu, na kupasa kuiamini na kumuamini Muhammad s.a.w. na kuisadiki Siku ya Kiyama. Na imekusudia kunabihisha watu wazingatie yaliyo wapata walio tangulia walio muasi Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na imeita watu washughulikie kuwafanyia wema wazazi wawili, na kuzitunza haki zao. Na hii Sura imeelezea kisa cha baadhi ya majini waliyo isikia Qur'ani tukufu, wakaambizana waisikilize. Wakaiona kuwa inathibitisha yale yale waliyo kuja nayo Mitume wa kabla ya Muhammad s.a.w., inaongoa kwendea Haki na kwenye Njia Iliyo Nyooka. Wakaiamini; na wakawataka wenzao wafuate yale yale. Ikamalizikia hadithi kwa wito wa kumtaka Nabii s.a.w. avumilie vile anavyo kadhibishwa na kaumu yake, na kumliwaza katika hayo kwa waliyo yastahamia Mitume wa kabla yake wenye azma ngumu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. H'A MIM¹

2. Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.²

3. Hatukuziumba mbingu na ardhi wala yaliyomo baina yake ila kwa haki na kwa muda maalumu. Na walio kufuru wanayapuuza yale wanayo onywa.³

4. Sema : Je! Mwawaona wale mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu? Nionyesheni wameumba nini katika ardhi; au hao wanayo shirika katika mbingu? Nileteeni Kitabu kilicho kuwa kabla ya hiki, au alama yoyote ya ilimu, ikiwa mnasema kweli.⁴

5. Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanao waomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao.⁵

6. Na ambao watu watakapo kusanywa watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.⁶

1 Imeanzia Sura hii kwa baadhi ya harufi kama ilivyo ada ya Qur'ani katika Sura kadhaa wa kadhaa.

2 Hii Qur'ani imeteremka kutokana na Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye hikima katika ayatendayo.

3 Hatukuziumba mbingu na ardhi na vyote vilio baina yake ila kufuatana na sharia zilizo thibiti, kwa makusudio yanayo ambatana na hikima, na kwa muda maalumu ambao baada yake utakwisha. Na wale wanao ukataa ukweli huu wanapuuza yale waliyo onywa kwayo, ya kuumbwa kupya siku watakapo fufuliwa watu kwa ajili ya malipo.

4 Waambie hao wanao muomba asiye kuwa Mwenyezi Mungu: Hebu nambieni hali ya hao mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu. Nijuvyeni wameumba nini katika ardhi, au wana ushirika wowote katika mbingu? Nileteeni Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu, au mabaki yoyote kutokana na ilimu za watu wa zamani ambayo mnayategemea kwa madai yenu, ikiwa mnasema kweli.

5 Na nani aliye zidi kupotea kuliko anaye muacha Mwenyezi Mungu akaiomba miungu mingine ambayo haitamjibu kitu mpaka mwisho wa dunia, na ambao hao hata hawana khabari ya maombi yao.

6 Na watu wakikusanywa kwa ajili ya hisabu Siku ya Kiyama hawa wanao abudiwa kwa upotovu watakuwa ndio maadui wa walio kuwa wakiabudu, na watajitenga nao, na kuwakadhibisha kwa madai yao kwamba wao wanastahiki kuabudiwa. (Katika Injili ya Mathayo inasimuliwa wazi vipi Nabii Isa

7. Na wanapo somewa Aya zetu zilizo wazi, walio kufuru husema juu ya haki inapo wajia: Huu ni uchawi dhaahiri.⁷
8. Au wanasema: Ameizua mwenyewe! Sema: Ikiwa nimeizua mimi, basi nyinyi hamwezi kunifaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Yeye anajua zaidi hayo mnayo ropokwa; anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi. Na Yeye ndiye Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁸
9. Sema: Mimi si kiroja miongoni mwa Mitume. Wala sijui nitakavyo fanywa wala nyinyi. Mimi nafuata niliyo funuliwa tu kwa Wahyi, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji mwenye kudhihirisha wazi.⁹
10. Sema: Mwaonaje yakiwa haya ni kweli yametoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi mmeyakataa, na akashuhudia shahidi miongoni mwa Wana wa Israili juu ya mfano wa haya, na akaamini, na nyinyi mnaofanya kiburi? Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu.¹⁰
11. Na walio kufuru waliwaambia walio amini: Lau kuwa hii ni kheri, wasingeli tutangulia. Na walipo kosa kuongoka wakasema: Huu ni uzushi wa zamani.¹¹
12. Na kabla yake kilikuwapo Kitabu cha Musa, kuwa chenye uwongozi na rehema. Na hichi ni Kitabu cha kusadikisha na kilicho kuja kwa lugha ya Kiarabu, ili kiwaonye walio dhulumu, na kiwe ni bishara kwa watendao mema.¹²
13. Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu; kisha wakatengenea,

a.s. atavyo wakataa Wakristo wanao muabudu yeye. Tazama Mathayo 7.22-23. Yesu anasema: “Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.”)

7 Na washirikina wakisomewa Aya zetu zilizo wazi wao husema, kwa ule ukafiri wao na inadi yao, bila ya kuzingatia, kuzisema hizo Aya: Huu ni uchawi dhaahiri!

8 Bali wanasema hawa makafiri: Muhammad ameizua hii na akamsingizia Mwenyezi Mungu! Sema kuwajibu: Ikiwa mimi nimeizua hii Mwenyezi Mungu atanipatiliza upesi upesi, wala nyinyi hamwezi kunilinda hata kwa chembe ya adhabu. Yeye peke yake ndiye Mwenye kujua kabisa hayo mnayo ropokwa katika kuzitia kombo Aya zake. Na Yeye anatosha kunishuhudia ukweli wangu, na kukushuhudilieni nyinyi kuwa mnanikadhibisha. Na Yeye pekee, ndiye Mkunjufu wa msamaha kwa mwenye kutubu, Mkubwa wa rehema, kwa kuwapa muhula wenye kuasi ili wadiriki kurejea.

9 Waambie: Mimi sikuwa Mtume wa mwanzo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hata ndio muukataa ujumbe wangu. Wala mimi sijui Mwenyezi Mungu atanifanya nini na atakufanyeni nini nyinyi. Mimi sifupati ninayo sema au kutenda ila anayo nifunulia Mwenyezi Mungu. Wala mimi si chochote ila ni mwonyaji miongoni mwa waonyaji.

10 Sema: Hebu nambieni, ikiwa hii Qur’ani inatoka kwa Mwenyezi Mungu na nyinyi mkaikataa, na hali ameshuhudia shahidi katika Wana wa Israili kuwa imeshuka mfano wa hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu, akawa yeye kaamini na nyinyi mkatakabari, basi hapo nyinyi si mtakuwa ni wenye kupotea na wenye kujidhulumu wenyewe kuliko watu wote? Hakika Mwenyezi Mungu hamsaidii kuongoka mwenye kujidhulumu mwenyewe na akapanda kiburi kuikataa Haki.

11 Na walio kufuru walisema kuwakhusu walio amini, kwa kejeli na majivuno juu yao: Ingeli kuwa aliyo kuja nayo Muhammad ni ya kheri, basi wasingeli tutangulia hawa katika kuyaamini. Kwani sisi ndio twenye ubwana, na akili bora! Na ilivyo kuwa hawakuyafuata basi wakaangukia kuyatoa kombo, wakisema: Huu ni uwongo wa zamani unatokana na hadithi za watu wa kale!

12 Na kabla ya Qur’ani Mwenyezi Mungu aliteremsha Taurati kuwa ni uwongozi na rehema kwa wenye kuitenda. Na hii Qur’ani wanayo ikadhibisha inasadikisha Vitabu vilivyo kwisha tangulia. Mwenyezi Mungu ameiteremsha kwa lugha ya Kiarabu iwe ni onyo jipya kwa wenye kudhulumu, na bishara kwa wenye kusimama sawa juu ya Njia.

hawatakuwa na khofu, wala hawatahuzunika.¹³

14. Hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo, kuwa ni malipo kwa waliyo kuwa wakiyatenda.¹⁴

15. Na tumemuusia mwanaadamu awatendee wema wazazi wake wawili. Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu, na akamzaa kwa taabu. Na kuchukua mimba kwake hata kumwachisha ziwa ni miezi thalathini. Hata anapo fika utu uzima wake, na akafikilia miaka arubaini, husema: Mola wangu Mlezi! Niwezeshe nishukuru neema zako ulizo nineemesha mimi na wazazi wangu, na nitende mema unayo yapenda. Na unitengenezee dhuriya zangu. Hakika mimi nimetubu kwako, na mimi ni miongoni mwa Waislamu.¹⁵

16. Hao ndio tunao wapokelea bora ya vitendo vyao walivyo vitenda, na tunayasamehe makosa yao. Watakuwa miongoni mwa watu wa Peponi. Miadi ya kweli hiyo walio ahidiwa.¹⁶

17. Na ambaye amewafyonya wazazi wake na akawaambia: Ati ndio mnanitisha kuwa nitafululiwa, na hali vizazi vingi vimekwisha pita kabla yangu! Na hao wazazi humwomba msaada Mwenyezi Mungu (na humwambia mtoto wao): Ole wako! Amini! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Na yeye husema: Hayakuwa haya ila ni visa vya watu wa kale.¹⁷

18. Hao ndio ambao imehakikishwa hukumu juu yao kama mataifa yaliyo kwisha pita kabla yao miongoni mwa majini na watu. Hakika hao wamekuwa wenye kukhasiri.¹⁸

19. Na wote watakuwa na daraja zao mbali mbali kwa waliyo yatenda, na ili awalipe kwa vitendo vyao, na wala hawatadhulumiwa.¹⁹

13 Hakika wanao sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu peke yake, kisha wakatengeneza kwa kufanya vitendo vizuri, watu hao hawana khofu ya kushukiwa la karaha, na wala hawatahuzunika kwa kuyakosa wayatakayo.

14 Hao wanao sifika kwa kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja, na kusimama sawa, ndio walio khusika kuingia Peponi wakikaa humo milele. Mwenyezi Mungu amewapa hayo kuwa ni jaza yao kwa mema waliyo kuwa wakiyatenda.

15 Na tumemuusia mwanaadamu kwa wazazi wake awafanyie wema mkubwa. Kwani mama yake amechukua mimba yake kwa mashaka, na akamzaa kwa mashaka. Na muda wa kuchukuliwa mimba mpaka kuachishwa ziwa ni miezi thalathini. Muda wote huo mama kapitikiwa na kila namna ya machungu. Mpaka huyo mtu alipo fikilia ukamilifu wa nguvu zake na akili yake, na akafikia miaka arubaini, husema: Mola wangu Mlezi! Nijaalie niishukuru neema yako uliyo nineemesha mimi na wazazi wangu, na nijaalie nitende vitendo vyema utavyo viridhi Wewe, na ujaalie huo wema wapate pia dhuriya zangu. Hakika mimi nimetubu kwako kwa kila dhambi, na mimi ni miongoni wa Waislamu, yaani walio zisalimisha nafsi zao kwako. (*Tazama Maelezo 46:15*)

16 Hao walio sifika kwa sifa hizo ndio tutakao wapokelea a'mali zao njema, na tutawasamehe maovu yao miongoni mwa watu wa Peponi. Itawahibitikia miadi ya kweli walio kuwa wakiahidiwa duniani.

17 Na waliwafyonya wazazi wao kwa kuchukua na kuchoka nao, walipo wataka waamini kufufuliwa, na wakawaambia: Mnaniambia tutatoka makaburini na mataifa mangapi yamepita kabla yangu na hapana hata mmoja aliye fufuliwa kutoka makaburini? Na hao wazazi wake wanaomba msaada kwa Mwenyezi Mungu jinsi ya kuona ni makuu makosa ya mwana wao, wakisema kwa kumshikilia aamini: Utaangamia wewe kama hukuamini. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kufufua ni kweli. Naye bado amekakamia kukadhibisha kwa kusema: Hayo mnayo yasema si chochote ila ni hadithi za uwongo za watu wa kale!

18 Hao wasemao hayo ndio iliyo wathibitikia kuwashukia adhabu sawa sawa na mataifa yaliyo kuwa kabla yao miongoni mwa majini na watu, kwa sababu hakika hao walikuwa ni wenye kukhasiri.

19 Na wote, Waislamu na makafiri, wana vyeo vyao vinavyo lingana na vitendo vyao walivyo vitenda,

20. Na siku watakapo letwa walio kufuru kwenye Moto wataambiwa: Nyinyi mlitwaa vitu vyenu vizuri katika uhai wa duniani, na mkastareheshwa navyo. Basi leo ndio mnalipwa adhabu ya fedheha kwa mlivyo kuwa mkitakabari katika ardhi bila ya haki, na kwa sababu mlikuwa mkifanya upotovu.²⁰

21. Na mtaje ndugu wa kina A'di, alipo waonya watu wake kwenye vilima vya mchanga. Na kwa yakini waonyaji wengi walitokea kabla yake na baada yake kuwaambia: Msimuabudu isipo kuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi nakukhofieni isikupateni adhabu ya siku iliyo kuu.²¹

22. Wakasema: Je! Umetujia ili ututenge mbali na miungu yetu? Basi tulettee hayo unayo tuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.²²

23. Akasema: Hakika ujuzi uko kwa Mwenyezi Mungu. Mimi nakufikishieni niliyo tumwa. Lakini nakuoneni kuwa nyinyi mnafanya ujinga.²³

24. Basi walipo liona wingu likielekea kwenye mabonde yao, walisema: Wingu hili la kutunyeshea mvua! Kumbe sivyo, haya ni hayo mliyo yahimiza, upepo ambao ndani yake imo adhabu chungu!²⁴

25. Unaangamiza kila kitu kwa amri ya Mola wake Mlezi. Wakawa hawaonekani ila nyumba zao tu. Hivyo ndivyo tuwalipavyo wakosefu!²⁵

26. Na bila ya shaka tuliwaweka vizuri sio kama tulivyo kuwekeni nyinyi; na tuliwapa masikio, na macho, na nyoyo. Na hayakuwafaa kitu masikio yao, wala macho yao, wala nyoyo zao kwa lolote. Kwani hao walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na yale waliyo kuwa wakiyafanyia maskhara ndiyo yakawazunguka.²⁶

ili uadilifu wa Mwenyezi Mungu upate kuonekana kati yao, na ili awalipe jaza ya 'amali zao, nao hawatadhulumiwa, kwa sababu wanastahiki hayo wanayo lipwa.

20 Na siku watakapo simamishwa walio kufuru kwenye Moto waambiwe: Mmekwisha chukua fungu lenu la vitu vizuri katika maisha yenu ya duniani, na mkavionea raha. Basi leo ndio mnalipwa adhabu ya kufedhehesha kwa mliyo kuwa nayo duniani, ya kujivuna katika nchi bila ya haki, na kutoka kwenye ut'iifu wa Mwenyezi Mungu.

21 Mtaje Hud, mwenzao kabila ya A'di, alipo wahadharisha watu wake wanao kaa Ah'qaaf, kwenye vilima vya mchanga. Na Mitume kadhaa walikuja kabla yake na baada yake kwa maonyo kama yake ya kusema: Msimuabudu ila Mwenyezi Mungu. Mimi nakukhofieni isikupateni adhabu yenye vitisho vikuu. (*Tazama Maelezo 46:21*)

22 Kaumu ya Hud walisema kwa kumkanya: Hivyo ndio umetujia ili utuachishe kuwaabudu miungu yetu? Basi tulettee hiyo adhabu ikiwa wewe hakika ni mwenye kusema kweli kwa ahadi hiyo.

23 Hud akasema: Ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kujua wakati wa kuileta adhabu yenu. Mimi nafikisha ujumbe tu nilio tumwa. Lakini naona kuwa nyinyi hamjui chochote katika mambo wanayo tumwa Mitume.

24 Ikawajia adhabu kwa sura ya wingu. Walipo liona limetanda kote juu linaelekea mabondeni kwao, walisema kwa furaha: Wingu hili linatuletea mvua na kheri. Wakaambiwa: Bali hilo ni hayo mliyo yahimiza, nayo ni upepo wenye adhabu kali na chungu, itakayo teketeza kila kitu kwa amri ya Muumbaji wake. Nao ukawaangamiza, yasionekane mabaki yao isipo kuwa nyumba zao. Hivyo ndivyo tunavyo mlipa kila mwenye kutenda kama makosa yao.

25 Tazama tanbihi ya 24.

26 Na tuliwaweka kabila la A'di kwa nafasi na nguvu sio kama tulivyo kuwekeni nyinyi watu wa Makka. Na tuliwajaalia masikio, na macho, na nyoyo, lau wangelitaka kunafiika kwayo. Lakini hayakuwafaa hata kitu kidogo masikio yao, wala macho yao, wala nyoyo zao, kwa sababu walikuwa wakizikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu. Basi hayo yakapinga baina yao na kunafiika kwa waliyo letewa. Na ile ile adhabu waliyo kuwa wakiifanyia maskhara ikawazunguka.

27. Na hakika tuliangamiza miji ilio jirani zenu, na tulizitumia Ishara ili wapate kurejea.²⁷

28. Basi mbona wale walio washika badala ya Mwenyezi Mungu, kuwa ati hao ndio wawakurubishe, hawakuwanusuru? Bali waliwapotea! Na huo ndio uwongo walio kuwa wakiuzua.²⁸

29. Na wakati tulipo waleta kundi la majini kuja kwako kusikiliza Qur'ani. Basi walipo ihudhuria walisema: Sikilizeni! Na ilipo kwisha somwa, walirudi kwa kaumu yao kwenda kuwaonya.²⁹

30. Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi tumesikia Kitabu kilicho teremshwa baada ya Musa, kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake, na kinacho ongoza kwenye Haki na kwenye Njia Iliyo Nyooka.³⁰

31. Enyi kaumu yetu! Muitikieni Mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu, na muaminini, Mwenyezi Mungu atakusameheni, na atakuingeni na adhabu chungu.³¹

32. Na wasio mwitikia Mwitaji wa Mwenyezi Mungu basi hao hawatashinda katika ardhi, wala hawatakuwa na walinzi mbele yake. Hao wamo katika upotovu ulio dhaahiri.³²

33. Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, aliye ziumba mbingu na ardhi, na hakuchoka kwa kuziumba, kuwa ni Muweza wa kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.³³

34. Na siku watakapo letwa makafiri Motoni wakaambiwa: Je! Haya si kweli? Watasema: Kwani? Tunaapa kwa Mola wetu Mlezi, ni kweli! Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya kule kukataa kwenu.³⁴

27 Enyi watu wa Makka! Tumeiangamiza miji iliyo jirani zenu. Na Sisi tuliwawekea wazi dalili namna mbali mbali, ili wapate kurejea waache ukafiri. Hawakurejea.

28 Basi kwani hao walio wafanya miungu badala ya Mwenyezi Mungu ili iwakaribishe kwa Mwenyezi Mtukufu imeweza kuwakinga na maangamizo? Hasha! Bali miungu hiyo iliwakimbia, na hali wao ndio wana haja nayo mno iwanusuru. Na hayo yaliyo wafika, ya kutupwa na miungu yao, na kuwapotea ndio matokeo ya uwongo wao na uzushi wao.

29 Ewe Muhammad! Taja tulipo kuletea kikundi cha majini waje sikiliza Qur'ani. Walipo hudhiria ilipo kuwa ikisomwa, baadhi yao wakawaambia wenzao: Sikilizeni! Ilipo kwisha timia kusomwa wakarudi kwa haraka kwa wenzao, kuwahadharisha na ukafiri, wakiwataka waamini.

30 Walisema: Enyi watu wetu! Hakika sisi tumekisikia Kitabu chenye shani kubwa. Kimeteremshwa baada ya Musa, na kinasadikisha Vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyo tangulia, kinaongoza kwenye itikadi ya haki, na sharia ya vitendo iliyo simama sawa.

31 Enyi watu wetu! Muitikieni mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu anaye ongoza kwenye Haki na kwenye Njia Iliyo Nyooka. Na msadikini Mwenyezi Mungu akusameheni madhambi yenu yaliyo tangulia, na akulindeni na adhabu kali iliyo chungu.

32 Na asiye mwitikia Mwenyezi Mungu basi hawezi kumshinda Mwenyezi Mungu asimtie mkononi hata akikimbia vipi katika ardhi. Na wala hana isipo kuwa Mwenyezi Mungu wa kumnusuru na kumkinga na adhabu yake. Hao wanao puuza wasimwitikie mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu wamo katika ubabaishi na dhaahiri wako mbali na Haki.

33 Wameghafilika wala hawajui kwamba Mwenyezi Mungu aliye ziumba mbingu na ardhi, na wala hakushindwa kuziumba, ni Muweza wa kuwafufua maiti? Bali Yeye ni Muweza wa hayo, kwani Yeye Mtukufu ana uweza kaamili juu ya kila kitu.

34 Na siku watakapo simamishwa walio kufuru Motoni wataambiwa kwa kukemewa: Adhabu hii si jambo la kweli linakubaliana na tuliyo kuonyeni nayo duniani? Na wao watasema: Kwani? Tunaapa kwa Mola wetu Mlezi, haya ni haki kweli. Atasema: Onjeni kila namna ya adhabu kali kwa kushikilia kwenu

35. Basi subiri, kama walivyo subiri Mitume wenye stahmala kubwa, wala usiwafanyie haraka. Siku watakayo yaona waliyo ahidiwa itakuwa kama kwamba hawakukaa ulimwenguni ila saa moja ya mchana. Huu ndio ufikisho! Kwani huangamizwa wengine isipo kuwa walio waovu tu?³⁵

ukafiri na ukanushi

35 Ewe Muhammad! Wastahamilie makafiri kama walivyo stahamili Mitume wengine wenye nguvu na imara wakati wa shida. Wala usiwahimizie adhabu. Kwani hiyo itawafika tu, hapana hivi wala hivi, hata ikichukua muda mrefu. Siku watapo kiona kitisho chake watadhani kuwa hawakukaa kabla yake ila saa moja tu ya mchana. Haya uliyo watolea waadhi yatosha. Hawataangamizwa kwa adhabu isipo kuwa walio toka kwenye ut'iifu.

Sura 47 - Muh'ammad

Utangulizi

Sura hii imeanza mwanzo wake kubainisha kwamba Mwenyezi Mungu amezibat' ilisha a'mali za makafiri kwa kuwa wamefuata upotovu, na amewafutia Waumini maovu yao kwa kufuata kwao Haki. Kama ilivyo eleza kwa urefu waajibu wa kuitetea Haki. Na malipo hayo kwa Akhera ni kuingia Peponi. Na ikawahimiza Waumini wainusuru Dini ya Mwenyezi Mungu na wapigane kwa ajili yake. Na imeweka wazi kwamba wapotovu wakiacha Imani hufanya fisadi katika nchi na wakawatupa jamaa zao. Na inahadharisha juu ya wanaafiki kuwa pamoja na Waumini wakapeleleza siri zao wapate kuwavunja moyo. Na inawatishia wanaafiki kuwa yatachanwa mapazia yao wanayo jifichia, na Mtume wa Mwenyezi Mungu adhihirishe chuki zao. Na inawakataza Waumini wasiwe wanyonge katika kupambana na makafiri, na hali wao ndio watakao shinda, na Mwenyezi Mungu yu pamoja nao, na wala hatawanyima malipo ya kazi yao. Kisha Sura imekhitimisha kutaka watu watoe kwa sababu ya Sabili Llah, Njia ya Mwenyezi Mungu, na ikabainisha kwamba mwenye kufanya ubakhili katika hayo basi anajidhuru mwenyewe, na kwamba kuacha kufuata Haki inakuwa ndiyo sababu ya kuhiliki hao wenye kuacha na kuletwa kaumu nyengine zenye kuleta kheri.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Walio kufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, Yeye atavipotoa vitendo vyao.¹
2. Na walio amini, na wakatenda mema, na wakaamini aliyo teremshiwa Muhammad - nayo ni Haki iliyo toka kwa Mola wao Mlezi - atawafutia makosa yao na ataitengeneza hali yao.²
3. Hayo ni kwa sababu walio kufuru wamefuata upotovu, na walio amini wamefuata Haki iliyo toka kwa Mola wao Mlezi. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo wapigia watu mifano yao.³
4. Basi mnapo wakuta walio kufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe. Ndio hivyo. Na lau angeli taka Mwenyezi Mungu angeli washinda mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu akutieni mitihani nyinyi kwa nyinyi. Na walio uliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu hatazipoteza a'mali zao.⁴

1 Walio mkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakawazuilia watu wasiingie katika Uislamu, Mwenyezi Mungu amevivunja vyote walivyo vitenda.

2 Na walio amini, na wakatenda mema, na wakasadiki yaliyo teremshwa kwa Muhammad, nayo ni Haki iliyo toka kwa Mola wao Mlezi, atawafutia makosa yao, na atawatengeneza hali yao ya Dini na dunia.

3 Hayo ni kwa sababu walio kufuru wamefuata njia ya upotovu, na kwamba walio amini wamefuata njia ya Haki iliyo toka kwa Mola wao Mlezi. Kwa mfano kama huu wa kubainisha kwa uwazi ndio Mwenyezi Mungu anawaeleza watu hali zao ili wapate kuzingatia.

4 Mtapo kutana na walio kufuru katika vita basi wapigeni kwenye shingo zao, mpaka mtakapo wadhoofisha kwa wingi wa kuwauwa, basi tena wafungeni mateka. Tena ama waachilieni wende zao kwa wema na ihsani, baada ya kwisha vita, kwa kuwaachia bila ya fidia, au kwa fidia ya kutoa mali au kubadilishana

5. Atawaongoza na awatengezee hali yao.⁵
6. Na atawaingiza katika Pepo aliyu wajuulisha.⁶
7. Enyi mlio amini! Mkiinusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu.⁷
8. Na walio kufuru, basi kwao ni maangamizo, na atavipoteza vitendo vyao.⁸
9. Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyu yateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao.⁹
10. Kwani hawakutembea katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa walio kuwa kabla yao? Mwenyezi Mungu aliwaangamiza, na kwa makafiri hawa itakuwa mfano wa hayo.¹⁰
11. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walio amini. Na makafiri hawana mlinzi.¹¹
12. Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walio amini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake. Na walio kufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao.¹²
13. Na miji mingapi iliyo kuwa na nguvu zaidi kuliko mji wako huu ulio kutoa; nao tuliwateketeza na wala hawakuwa wa kuwanusuru.¹³
14. Je! Mwenye kuwa na bayana kutoka kwa Mola wake Mlezi ni kama aliye pambiwa uovu wa vitendo vyake, na wakafuata pumbao lao?¹⁴
15. Mfano wa Pepo walio ahidiwa wachamngu ina mito ya maji yasiyo vunda, na mito

kwa mateka wa Kiislamu. Inakuwa mmewaachilia kwa badali. Huu ndio uwe mwendo wenu na makafiri mpaka vita vimalizike kabisa. Mwenyezi Mungu anawahukumieni hivyo. Na lau angeli taka bila ya shaka angeli washinda bila ya vita, lakini haya ni ili awajaribu Waumini kwa makafiri kama mthani ndio ameamrisha Jihadi. Na walio uwawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kabisa hatoacha vitendo vyao vipotee. Atawahidi, na azitengeneze nyoyo zao, na awatie katika Pepo aliyu kwisha wajuulisha. (*Tazama Maelezo 47:4*)

5 Tazama tanbihi ya 4.

6 Tazama tanbihi ya 4.

7 Enyi mlio amini! Mkiinusuru Dini ya Mwenyezi Mungu, na Yeye atakunusuruni muwashinde maadui zenu, na ayatilie nguvu mambo yenu.

8 Na walio kufuru Mwenyezi Mungu atawatia mashakani, na atawapotoa vitendo vyao.

9 Mambo yao ni hivyo kwa sababu wao wanakereka na aliyu teremsha Mwenyezi Mungu, yaani Qur'ani na amri zake. Basi Mwenyezi Mungu ameivat'lisha vitendo vyao.

10 Wameshindwa kutafuta ya kuwazindua, hata hawakutembea katika ardhi wakaangalia hali gani ulikuwa mwisho wa walio wakadhibisha Mitume kabla yao? Mwenyezi Mungu aliwateremshia hilaki katika kila kilicho khusiana nao, nafsi zao, mali yao, na watoto wao. Na wenye kumkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake ndio hupata mwisho mfano wa huo.

11 Malipo hayo ndio ushindi wa Waumini na kushindwa nguvu makafiri, ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu ni rafiki mlinzi wa walio amini na ndiye Mwenye kuwanusuru; na makafiri hawana rafiki mlinzi wa kuwanusuru wala kuwakinga na kuangamia.

12 Hakika Mwenyezi Mungu atawatia wenye kuamini na wakatenda mema katika Pepo tukufu zenye kupitiwa ndani yake mito. Na makafiri wanastarehe duniani kidogo, na wanakula kama walavyo wanyama, wamepigwa na mghafala wala hawajifikirii mwisho wao. Hawanalo lao ila matamano yao. Na kesho Akhera nyumba yao ni Motoni.

13 Na wengi katika watu wa miji walio tangulia walio kuwa na nguvu zaidi kushinda watu wa mji wako wa Makka ambao watu wake wamekufukuza, ewe Muhammad, tuliwaangamiza kwa namna mbali mbali za adhabu. Na hakutokea yeyote wa kuwanusuru nasi.

14 Je! Wanaweza kuwa sawa makundi mawili haya katika malipo? Mwenye kuwa na ujuzi wazi kumjua Muumba wake na Mlezi wake, naye akawa anam'ii, atakuwa sawa na mwenye kuwa na vitendo vyake viovu naye akaviona ni vizuri, na akafuata hayo ayatendayo na akaeneza pumbao lake la upotovu.

ya maziwa isiyo haribika ladha yake, na mito ya mvinyo yenye ladha kwa wanywao, na mito ya asali iliyo safishwa. Na wao humo watakuwa na kila namna ya matunda, na maghfira kutoka kwa Mola wao Mlezi. Basi hao ni kama watakapo dumu Motoni na wakinyweshwa maji yanayo chemka ya kuwakata matumbo yao?¹⁵

16. Na wapo miongoni mwao wanao kusikiliza, mpaka wakiondoka kwako huwauliza walio pewa ilimu: Amesema nini sasa hivi? Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao, na wakafuata pumbao lao.¹⁶

17. Na wale walio ongoka anawazidishia uongofu na anawapa uchamngu wao.¹⁷

18. Kwani wanangojea jengine isipo kuwa iwafikie Saa (ya Kiyama) kwa ghafla? Na hakika alama zake zimekwisha kuja. Na itapo wajia kutawafaa wapi kukumbuka hapo?¹⁸

19. Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu, na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa.¹⁹

20. Na Waumini wanasema: Kwa nini haiteremshwi Sura? Na inapo teremshwa Sura madhubuti na ikatajwa ndani yake khabari ya vita, utawaona wenye maradhi katika nyoyo zao wanakutazama mtazamo wa anaye zimia kwa mauti. Basi ni bora kwao?²⁰

21. Ut'iifu na kauli njema. Na jambo likisha azimiwa, basi wakiwa ni wakweli kwa Mwenyezi Mungu, bila ya shaka itakuwa ni kheri kwao.²¹

22. Basi yanayo tarajiwa kwenu mkitawala ndio mfididi katika nchi na mwatupe jamaa zenu?²²

15 Sifa ya Pepo walio ahidiwa wachamngu ni kama hivi: ndani yake imo mito ya maji yasiyo chafuka, na mito ya maziwa yasiyo haribika utamu wake, na mito ya mvinyo yenye ladha kwa wanywao, na mito ya asali iliyo safishwa na takataka zote. Na humo watakuwa na kila namna ya matunda, na msamaha mkubwa kutokana na Mola wao Mlezi. Je! Sifa za Pepo ya hawa ni kama sifa itayo kuwa ni malipo ya mwenye kudumu milele Motoni, na akanyweshwa maji yaliyo tokota ya kukata matumbo? (*Tazama Maelezo 47:15*)

16 Na miongoni mwa makafiri kipo kikundi cha watu wanao kusikiliza wewe, Muhammad. Hawakuamini wewe, wala hawanafikiri na maneno yako. Mpaka wakisha ondoka kwenye baraza yako husema kwa kejeli kuwaambia walio pewa ujuzi: Kasema nini huyu Muhammad sasa hivi? Watu hao ndio Mwenyezi Mungu amepiga muhuri wa ukafiri juu ya nyoyo zao. Ndio wameiacha kheri wakifuata matamano yao.

17 Na walio ongoka wakashika njia ya Haki, Mwenyezi Mungu huwazidishia uongofu, na akawapa kinga chao cha kujikingia na Moto.

18 Wanao kanusha hawawaidhiki na hali za walio tangulia. Basi je! Wanangojea Saa (ya Kiyama) iwajie kwa ghafla? Kwa hakika alama zake zimekwisha dhihiri, na wao hawajazingatia kuwa inakuja. Basi watakumbuka wapi itapo wajia mara moja kwa ghafla?

19 Basi thibiti juu ya ujuzi ya kwamba hakika hapana wa kuabudiwa kwa Haki ila Mwenyezi Mungu tu. Na muombe maghfira Mwenyezi Mungu kwa dhambi yako na madhambi ya Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua kila lenu, la kupita na la kukaa.

20 Walio amini wanasema: Haiteremki Sura ya kututaka tupigane? Na ikiteremka Sura ambayo haifasiriki vyenginevyo ila ni kulazimisha tu, na ikataja ndani yake kuamrisha vita, utawaona ambao katika nyoyo zao mna unaafiki wanakuangalia kwa muangalio wa mwenye kuzimia kwa mauti, jinsi ya kuvigopa na kuvichukia vita. Linalo wastahikia kulifanya ni kumt'ii Mwenyezi Mungu na kusema neno linalo kubaliana na sharia. Na mambo yakawa ni kweli, na ikawalazimu kupigana, basi lau kuwa ni kweli wana Imani ya Mwenyezi Mungu na ut'iifu ingeli kuwa bora kwao kuliko huo unaafiki. Basi ndio mnavyo tarajiwa, enyi wanaafiki, kuwa mkipata madaraka ndio mfididi katika nchi na mkate makhusiano yenu na jamaa zenu?

21 Tazama tanbihi ya 20.

22 Tazama tanbihi ya 20.

23. Hao ndio Mwenyezi Mungu alio walaani, na akawatia uziwi, na akawapofoa macho yao.²³
24. Je! Hawazingatii hii Qur'ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?²⁴
25. Kwa hakika wanao rudi nyuma baada ya kwisha wabainikia uwongofu, Shetani huyo amewashawishi na amewaghuri.²⁵
26. Hayo ni kwa sababu waliwaambia walio chukia aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu: Tutakut'iini katika baadhi ya mambo. Na Mwenyezi Mungu anajua siri zao.²⁶
27. Basi itakuwaje Malaika watakapo wafisha wakawa wanawapiga nyuso zao na migongo yao!²⁷
28. Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyo mchukiza Mwenyezi Mungu na wakachukia yanayo mridhisha, basi akaviangusha vitendo vyao.²⁸
29. Je! Wenye maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hatazidhihirisha chuki zao?²⁹
30. Na tungeli penda tungeli kuonyesha hao na ungesi watambua kwa alama zao; lakini bila ya shaka utawajua kwa namna ya msemo wao. Na Mwenyezi Mungu anavijua vitendo vyenu.³⁰
31. Na bila ya shaka tutakujaribuni mpaka tuwadhihirishe wapignao Jihadi katika nyinyi na wanao subiri. Nasi tutazifanyia mtihani khabari zenu.³¹
32. Kwa hakika walio kufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu na wakapinzana na Mtume baada ya kwisha wabainikia uwongofu, hao hawatamdhuru Mwenyezi Mungu kwa lolote. Naye ataviangusha vitendo vyao.³²
33. Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume, wala msiviharibu

23 Hao ndio alio watenga mbali kabisa Mwenyezi Mungu na rehema yake, na akawatia uziwi wasiisikie Haki, na akawatia upofu wa macho wasiione Njia ya Uwongofu.

24 Wameingia upofu hata hawaufahamu uwongofu wa Qur'ani? Bali kwenye nyoyo zao zipo kufuli zinawazuia wasiizingatie.

25 Hakika wale walio ritadi, wakarejea nyuma kwenye ukafiri na upotofu walio kuwa nao baada ya kuwadhihirikia njia ya uwongofu, Shetani ndiye aliye wapambia, na akawakunjulia matamano ya uwongo.

26 Kurejea huko ukafirini ni kwa kuwa waliwaambia wenye kuchukia aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu: Tutakut'iini katika baadhi ya mambo. Na Mwenyezi Mungu anazijua siri za hawa wanaafiki. Hiyo ndiyo hali katika maisha ya duniani, basi watakuwa katika hali gani Malaika watapo wafisha huku wakiwapiga nyuso zao na migongo yao kwa kuwadhalilisha?

27 Tazama tanbihi ya 26.

28 Kufishwa namna hiyo ya kutisha katika hali hiyo ni kwa kuwa hakika wao waliufuata upotovu ulio mkasirisha Mwenyezi Mungu, na wakaichukia Haki inayo mpendeza Mwenyezi Mungu. Basi akayabat'ilisha waliyo yatenda.

29 Hivyo wanadhani hawa wenye unaafiki katika nyoyo zao kwamba Mwenyezi Mungu hatazifichua chuki zao wanazo mchukia Mtume wake na Waumini?

30 Tungeli penda bila ya shaka tungeli kuonyesha hao wanaafiki, nawe ungesi wajua kwa alama zao, na ungesi wajua kwa namna yao wanavyo sema. Na Mwenyezi Mungu anajua ukweli wa vitendo vyenu vyote.

31 Na ninaapa: Bila ya shaka tutakujaribuni kama kukufanyieni mtihani, mpaka tuwajue Mujaahidina, wanao pigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, katika nyinyi, na wenye kuvumilia wakati wa shida na dhiki, na tuzijue khabari zenu za ut'iifu na maasi katika Jihadi na penginepo.

32 Hakika walio kufuru na wakazuia njia ya Mwenyezi Mungu, na wakenda kinyume na Mtume kwa inda na ukaidi, baada ya kwisha wadhihirikia uwongofu, hao hawatamdhuru Mwenyezi Mungu kwa lolote. Na Yeye atayabat'ilisha yote waliyo yatenda.

vitendo vyenu.³³

34. Hakika walio kufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakafa na hali ni makafiri, Mwenyezi Mungu hatawasamehe makosa yao.³⁴

35. Basi msiregee na kutaka suluhu, maana nyinyi ndio mtakao shinda. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja nanyi, wala hatakunyimeni malipo ya vitendo vyenu.³⁵

36. Hakika uhai wa duniani ni mchezo na pumbao. Na mkiamini na mkamchamngu Mwenyezi Mungu atakupeni ujira wenu, wala hakutakeni mali yenu.³⁶

37. Na akikutakeni hayo na kukushikilieni mtafanya ubakhili, na atatoa undani wa chuki zenu.³⁷

38. Angalieni! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wapo katika nyinyi wanao fanya ubakhili. Na anaye fanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu si mhitaji, na nyinyi ndio wahitaji. Na mkiageuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi.³⁸

33 Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu katika aliyo kuamrisheni, na mt'iini Mtume kwa hayo anayo kuitieni, wala msivipoteze vitendo vyenu.

34 Hakika walio kufuru na wakazuia watu wasiingie katika Uislamu, kisha wakafa nao ni makafiri, basi Mwenyezi Mungu hatawasamehe.

35 Basi msijifanye wanyonge mbele ya maadui zenu mnapo kutana nao. Wala msiwatake suluhu kwa kuwaogopa, na hali nyinyi ndio mko juu, na ni wenye kushinda kwa nguvu za Imani. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja nanyi kwa nusra yake; na wala hatakupunguzieni malipo ya vitendo vyenu.

36 Hakika uhai wa dunia ni upotovu na udanganyifu. Na nyinyi mkiamini na mkaacha maasi, na mkafanya kheri, Mwenyezi Mungu atakupeni thawabu ya hayo, wala hakutakini mali yenu. Akikutakeni na akakushikilieni basi nyinyi mtafanya uchoyo, na chuki zenu zitaonekana kwa mnavyo yapenda mali.

37 Tazama tanbihi ya 36.

38 Hivi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu aliyo iamrisha. Kati yenu wapo wanao fanya ubakhili kutoa. Na mwenye kufanya ubakhili hamdhuru mtu ila nafsi yake. Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye tajiri, hana haja ya mtu, na nyinyi ndio mafakiri wenye kumhitajia Yeye. Na mkiacha kumt'ii Mwenyezi Mungu basi atakubadilisheni pahala penu awaleta watu wengine, tena hao hawatakuwa mfano wenu wa kuacha kumt'ii.

Sura 48 - Al-Fat'h

Utangulizi

Imeanzia mwanzo wake Sura hii kwa kutaja Ushindi ulio wazi, alio msahilishia Mwenyezi Mungu Mtume wake, na imeelezea athari zake kubwa katika kueneza Uislamu na kuwatukuza Waislamu, na kuziimarisha nyoyo za Waumini ili wazidi Imani, na kuadhibiwa kwa wanaafiki na washirikina, kwa shaka shaka zao juu ya nusura ya Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake. Na imetaja kuwa Mtume Muhammad s.a.w. ametumwa kuwa ni mwenye kushuhudia, na mwenye kubashiria, ili ithibiti Imani ya Mwenyezi Mungu. Tena Sura ikaingia kueleza kusimulia kuungwa mkono Mtume na watu wa kweli wa kutimiza ahadi, na ikabainisha uwongo wa udhuru walio toa walio kwenda kinyume na Mtume wasitoke naye kwenda pambana na maadui, na ambao walibaki nyuma kwa kudhania kwao kuwa Mwenyezi Mungu hatampa nusura Mtume, na ikaeleza kuwa kutaka kwao kutoka naye ni kwa sababu ya kupata ngawira. Tena Sura imebainisha kuwa watakuja takiwa kupigana na kaumu wakali na wenye nguvu, na kwamba hapana makosa kuacha kwenda vitani kwa udhuru wa kweli. Kama ilivyo weka wazi ukubwa wa kheri alizo waahidi Mwenyezi Mungu wale alio furahi nao katika kumuunga mkono Mtume s.a.w. kwa Ridhwani. Imezungumzia juu ya kukimbia kwao makafiri na kushindwa kwao walipo pigana na Waumini, ikaeleza hikima ya Mwenyezi Mungu kuwazuia makafiri wasiwapige Waumini, na kuwazuia Waumini wasiwapige makafiri wakati wa kutekwa Makka. Na mazungumzo yakamalizikia kwa kubainisha kwamba Mwenyezi Mungu ameitimiza ndoto aliyotea Mtume wake ya kuingia katika Msikiti Mtakatifu, na kwamba Muhammad na walio amini pamoja naye ni wakali kwa makafiri lakini ni wapole, wanaoneana huruma wao kwa wao. Na ikabainisha alama za kuwajuulisha Waumini, na sifa zao katika Taurati na sifa zao katika Injili, na Mwenyezi Mungu kawaahidi walio amini na wakatenda mema msamaha mkunjufu, na ujira mkubwa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Hakika tumekufungulia Ushindi wa dhaahiri¹
2. Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyo tangulia na yajayo, na akutimizie neema zake, na akuongoe katika Njia Iliyo Nyooka,²
3. Na Mwenyezi Mungu akunusuru nusura yenye nguvu -³
4. Yeye ndiye aliye teremsha utulivu katika nyoyo za Waumini ili wazidi Imani juu

1 Hakika Sisi tumekupa, ewe Muhammad, FAT'H, Ushindi mkubwa unao onekana wazi kwa Haki kuishinda baat'ili, kweli kuishinda uwongo, ili Mwenyezi Mungu akughufirie yaliyo tangulia katika yanayo hisabika kwa mwenye cheo kama chako kuwa ni dhambi, na pia yanayo kuja baada yake. Na ili atimize neema zake juu yako kwa kuenea wito wako, na akuthibitisha kwenye Njia ya Mwenyezi Mungu Iliyo Nyooka. Na Mwenyezi Mungu akunusuru na maadui wa Utume wako kwa nusura yenye nguvu za kushinda.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

ya Imani yao. Na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi, Mwenye hikima -⁴

5. Ili awaingize Waumini wanaume na Waumini wanawake katika Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo, na awafutie makosa yao. Na huko ndiko kufuzu kukubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.⁵

6. Na awape adhabu wanaafiki wanaume na wanaafiki wanawake, na washirikina wanaume na washirikina wanawake, wanao mdhania Mwenyezi Mungu dhana mbaya. Utawafikia mgeuko mbaya, na Mwenyezi Mungu awakasirikie, na awalaani, na awaandalie Jahannamu. Na hayo ni marudio maovu kabisa.⁶

7. Na Mwenyezi Mungu ana majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.⁷

8. Hakika tumekutuma wewe uwe Shahidi, na Mbashiri, na Mwonyaji,⁸

9. Ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mumsaidie, na mumhishimu, na mumtakase asubuhi na jioni.⁹

10. Bila ya shaka wanao fungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi hizi anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na anaye tekeleza aliyo muahadi Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamlipa ujira mkubwa.¹⁰

11. Watakuambia mabedui walio baki nyuma: Yametushughulisha mali yetu na ahali zetu, basi tuombe msamaha. Wanasema kwa ndimi zao yasiyo kuwamo katika nyoyo zao. Sema: Ni nani awezaye kukusaidieni chochote kwa Mwenyezi Mungu akitaka Yeye kukudhuruni au akitaka kukunufaisheni? Bali Mwenyezi Mungu anazo khabari

4 Yeye ndiye aliye teremsha utulivu katika nyoyo za Waumini ili wazidi kuwa na yakini juu ya yakini yao. Na ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye majeshi ye katika mbingu na ardhi. Huendesha mambo yake apendavyo. Na Mwenyezi Mungu amevizunguka vitu vyote kwa ujuzi wake. Ana hikima isiyo na ukomo katika kuendesha kila kitu.

5 Ili Mwenyezi Mungu awaingize Waumini wanaume na Waumini wanawake katika Mabustan, yaani Pepo, zipitiwazo na mito ndani yake, wadumu humo daima dawamu, na awafutie makosa yao. Na malipo hayo kwa Mwenyezi Mungu ndio kufuzu kulio fika ukomo kwa utukufu wake. Na ili awatie adhabu wanaafiki wanaume na wanaafiki wanawake, na wanaume wanao mshirikisha Mwenyezi Mungu na wengineo, na washirikina wa kike, wanao mdhania Mwenyezi Mungu dhana mbovu, ya kuwa ati hatamnusuru Mtume wake. Ni juu yao peke yao ndio yatawaangukia mageuko maovu, wala hawawezi kuyakimbia. Mwenyezi Mungu amewaghadhibikia, ne amewafukuza kwenye rehema yake, na amewatengenezea Jahannamu kwa ajili ya kuwaadhibu, na huo ndio mwisho mbaya.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Na Mwenyezi Mungu anayo majeshi ya mbinguni na katika ardhi. Anaendesha mambo yake kwa hikima yake kama atakavyo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye hikima isiyo na mwisho katika kupanga kila kitu.

8 Ewe Muhammad! Hakika Sisi tumekutuma uwe Shahidi juu ya umma wako na pia juu ya kaumu zilizo tangulia, na uwe Mbashiri kuwapa khabari njema wachamnгу kuwa watapata malipo mema, na uwe Mwonyaji kwa watandao maasi kuwa watapata adhabu mbaya.

9 Ili nyinyi, mlio tumiwa Mtume, mpate kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mumnusuru Mwenyezi Mungu kwa kuinusuru Dini yake, na mumtukuze kwa taadhima na utukufu, na mumtakase na kila lisilo muelekea, asubuhi na jioni.

10 Hakika wanao kuahidi kuwa watafanya kama wawezalo kukunusuru, kwa hakika wanamuahidi Mwenyezi Mungu. Nguvu za Mwenyezi Mungu ziko pamoja nawe juu ya nguvu zao. Basi atakaye vunja ahadi yake baada ya kwisha itoa, basi madhara yake hayatarudia ila juu ya nafsi yake. Na mwenye kutimiza ahadi aliyo muahidi Mwenyezi Mungu, kwa kutimiza kufungamana nawe, Mwenyezi Mungu atamlipa thawabu za hadi ya mwisho wa ukubwa.

za mnayo yatenda.¹¹

12. Lakini mlidhani kwamba Mtume na Waumini hawatarudi kabisa kwa ahali zao, na mkapambiwa hayo katika nyoyo zenu, na mkadhanja dhana mbaya, na mkawa watu wanao angamia.¹²

13. Na asiye muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi kwa hakika Sisi tumewaandalia makafiri Moto mkali.¹³

14. Na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Humsamehe amtakaye, na humuadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.¹⁴

15. Walio baki nyuma watasema: Mtapo kwenda kuchukua ngawira, tuacheni tukufuateni! Wanataka kuyabadili maneno ya Mwenyezi Mungu. Sema: Hamtatufuata kabisa. Mwenyezi Mungu alikwisha sema kama hivi zamani. Hapo watasema: Bali nyinyi mnatuhusudu. Siyo, bali walikuwa hawafahamu ila kidogo.¹⁵

16. Waambie walio achwa nyuma katika mabedui: Mtakuja itwa kwenda pigana na watu wakali kwa vita, mpigane nao au wasalimu amri. Basi mkimt'ii, Mwenyezi Mungu atakupeni ujira mzuri. Na mkigeuka kama mlivyo geuka kwanza, atakuadhibuni kwa adhabu iliyo chungu.¹⁶

17. Kipofu hana lawama, wala kiguru hana lawama, wala mgonjwa hana lawama. Na mwenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, atamuingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Na atakaye geuka upande atamuadhibu kwa adhabu chungu.¹⁷

11 Watakwambia hao walio wekwa nyuma na unaafiki wao katika wakaazi wa majangwani, utapo rejea kutoka safarini: Yametushughulisha mali yetu na ahali zetu hata hatukuweza kutoka nawe. Basi tuombe maghira. Wanasema hayo kwa ndimi zao yasiyo kuwamo katika nyoyo zao. Sema kuwajibu: Nani anaye weza kukufanyieni chochote kukulindeni na hukumu ya Mwenyezi Mungu, pindi akitaka kukudhuruni, au akitaka kukufaeni? Bali Mwenyezi Mungu amevizunguka vyote mtendavyo kwa ujuzi wake.

12 Bali nyinyi mlidhani kwamba Mtume na Waumini hawatarejea kabisa kwa watu wao baada ya vita vyao. Ndio maana mkabaki nyuma, na mkadanganyika na hiyo dhana katika nyoyo zenu. Na mkadhanja dhana mbovu katika mambo yenu yote. Na Mwenyezi Mungu alikwisha jua kuwa nyinyi ni watu walio angamia, wenye kustahiki ghadhabu zake.

13 Na asiye muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi Sisi tumewatengenezea makafiri Moto unao waka kwa nguvu.

14 Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye ufalme wa mbinguni na katika ardhi, anaupanga kwa mpango wa Mwenye uweza, Mwenye hikima. Humsamehe madhambi amtakaye, na humuadhibu kwa hikima yake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mkuu wa kusamehe, Mkunjufu wa rehema.

15 Watasema kwa wakaazi wa majangwani walio wekwa nyuma na unaafiki wastoke nawe: Mkenda kuchukua ngawira, aliyo kuahidini Mwenyezi Mungu kuzichukua, twacheni takufuateni. Hao wanataka kuigeuza ile ahadi ya Mwenyezi Mungu juu ya ngawira hizo aliyo wapa waliotoka na Mtume kwenda Hudaibiya. Ewe Muhammad! Waambie: Hamtafuata. Hukumu kama hiyo ya kuzuwia kufuata Mwenyezi Mungu aliihukumia kabla ya hapo kwa mintarafu ya ngawira kwa walio toka kwenda vitani pamoja na Mtume wake. Wao watasema: Mwenyezi Mungu hakukuamrisheni hayo, bali nyinyi mnatuhusudu tu, hamtaki tushirikiane nanyi. Bali watu hawa, kwa haya wayasemayo, hawafahamu sharia za Mwenyezi Mungu ila kwa fahamu chache.

16 Waambie walio baki nyuma wasitoke katika watu wa majangwani. Mtakuja takiwa kwenda pigana na watu wa kali wa vita. Ikiwa mtaitikia wito huo basi hapo Mwenyezi Mungu atakupeni ngawira nyingi katika dunia, na thawabu katika Akhera. Na mkikataa kama mlivyo kwisha kataa kabla, besa Mwenyezi Mungu atakuadhibuni kwa adhabu ya mwisho wa uchungu.

17 Kipofu hapati dhambi kuacha kwenda pigana na makafiri, wala kiguru hapati dhambi, wala mgonjwa hapati dhambi kadhaalika. Kwani hao hawajiwezi. Na mwenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake katika kila anacho amrisha na kukataza, atamtia katika Mabustani ya Peponi yenye wasaa, yapitayo mito kati yake. Na mwenye kuacha kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bass Yeye atamuadhibu

18. Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waumini walipo fungamana nawe chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawalipa kwa Ushindi wa karibu.¹⁸

19. Na ngawira nyingi watakazo zichukua. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹⁹

20. Mwenyezi Mungu anakuahidini ngawira nyingi mtakazo zichukua, basi amekutangulizieni hizi kwanza, na akaizuia mikono ya watu isikufikieni, na ili hayo yawe ni Ishara kwa Waumini, na akakuongozeni Njia Iliyo Nyooka.²⁰

21. Na mengine hamwezi kuyapata bado, Mwenyezi Mungu amekwisha yazingia. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.²¹

22. Na lau makafiri wangeli pigana nanyi basi bila ya shaka wangeli geuza migongo, kisha wasingeli pata mlinzi wala msaidizi.²²

23. Huo ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu ulio kwisha pita zamani, wala hutapata mabadiliko katika mwendo wa Mwenyezi Mungu.²³

24. Na Yeye ndiye aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya kukupeni Ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona myatendayo.²⁴

25. Hao ndio walio kufuru na wakakuziieni msiingie Msikiti Mtakatifu, na wakawazuilia dhabihu kufika mahala pao. Na lau si wanaume Waumini na wanawake Waumini msio wajua mkawasaga na mkaingia makosani kutokana nao bila ya kujua. Mwenyezi Mungu (amefanya haya) ili amuingize amtakaye katika rehema yake. Lau wangeli tengana bila ya shaka tungeli waadhibu walio kufuru kwa adhabu chungu.²⁵

adhabu iliyo chungu hadi.

18 Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waumini walipo kuahidi kwa kujitolea chini ya mti. Yeye alijua yaliyomo katika nyoyo zao, ya ikhlasi na kuutiliza Ujumbe wako. Basi akawateremsha utulivu, na kwa ajili ya ukweli wao katika kukuunga mkono na kutimiza sulhu aliwapa nguvu hapo hapo, na ngawira nyingi alizo waahidi kuwa watazipata. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye hikima ya mwisho katika kila analo lihukumia.

19 Tazama tanbihi ya 18.

20 Mwenyezi Mungu amekuhidini ngawira nyingi mtakazo chukua katika wakati ulio kadiriwa kwa hayo. Basi akakuleteeni haraka haraka. Na hayo ndiyo hizo ngawira alizo kuahidini. Na akakuingeni na madhara ya watu juu yenu. Na ili hayo yawe ni Ishara kwa Waumini juu ya ukweli wa ahadi ya Mwenyezi Mungu kwao, na akuongozeni kwenye Njia Iliyo Nyooka, kwa kumt'ii Yeye na kumfuata Mtume wake. Na ngawira nyengine ambazo mlikuwa hamjazipata Mwenyezi Mungu amekupeni ushindi wa kuzipata. Na Mwenyezi Mungu ana uwezo ulio timia juu ya kila kitu.

21 Tazama tanbihi ya 20.

22 Na lau makafiri wa Makka wangeli pigana nanyi, na wasifanye ile sulhu nanyi, basi wangeli toka mbio kwa kushindwa, kwa kukuogopeni, na tena hapo wasinge pata mlinzi wowote wa kuwatawalia mambo yao, wala mtu wa kuwanusuru.

23 Mwenyezi Mungu ameendesha mambo yake kwa mwendo kama alio uendesha zamani kwa viumbe vyake - nayo ni kuwa khatima njema ni ya Mitume wake na Waumini. Wala hutakuta mabadiliko katika mwendo wa Mwenyezi Mungu.

24 Na huyo ni Mwenyezi Mungu pekee, ndiye aliye izuia mikono ya makafiri isikudhuruni katika vita vyao kati ya Makka. Na baada yake akakupeni uwezo wa kuwashinda. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona yote myatendayo.

25 Watu wa Makka ndio walio kufuru na wakakuziilieni msiingie katika Msikiti Mtakatifu, na wakawazuilia dhabihu wanyama wa kutoa mhanga mlio wachunga na kuwafunga kwa ajili ya kutoa dhahiya, wasifike pahala pao pa kuchinjiwa. Na lau kuwa si ubaya wa kuwasibu Waumini wanaume na wanawake kati ya makafiri wa Makka, ambao hamwajui, mkawauwa bila ya kuwajua, na mkapata a'ri

26. Pale walio kufuru walipo tia katika nyoyo zao hasira, hasira za kijinga, Mwenyezi Mungu aliteremsha utulivu juu ya Mtume wake na juu ya Waumini, na akawalazimisha neno la kuchamngu. Na wao walikuwa ndio wenye haki nalo na wenye kustahili. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.²⁶

27. Hakika Mwenyezi Mungu amementimizia Mtume wake ndoto ya haki. Bila ya shaka nyinyi mtaungia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, kwa amani, na hali mmenyoa vichwa vyenu na mmpunguza nywele. Hamtakuwa na khofu. Yeye anajua msiyo yajua. Basi atakupeni kabla ya haya Ushindi karibuni.²⁷

28. Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya Haki, ili aitukuze juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi.²⁸

29. Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama na kusujudu wakitafuta fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili ni kama mmea ulio toa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya ubuwa wake, ukawafurahisha wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri. Mwenyezi Mungu amewaahidi walio amini na wakatenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa.²⁹

na hizaya kwa ajili ya kuwauwa, basi tungeli kusalitisheni nao mkapambana nao. Na kuzuliwa huko ni kwa ajili ya kuwa Mwenyezi Mungu apate kuwaingiza katika ulinzi wake Waumini walio baina yao, na walio silimu miongoni mwa makafiri. Lau kuwa wanatambulikana Waumini basi tungeli waadhibu walio shikilia ukafiri kati yao adhabu ya ukomo wa uchungu, pale wale walio kufuru walipo fanya katika nyoyo zao dharau za kijahiliya basi Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu juu ya Mtume wake na juu ya Waumini, na akawalazimisha neno la kujikinga na ushirikina na adhabu. Na wao walikuwa ni wenye kustahiki na kuelekea hayo, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.

26 Tazama tanbihi ya 25.

27 Ameitimiza Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake ile ndoto ya Mtume kwa kuingia Msikiti Mtakatifu kwa hakika. Ninaapa: Hapana shaka mtaungia katika Msikiti Mtakatifu, Mwenyezi Mungu akipenda, nanyi mmesalimika na maadui zenu, na huku ni wenye kunyoa na kupunguza nywele zenu, na bila ya khofu. Mwenyezi Mungu *Subhanahu* anajua kheri msiyo ijua kwa kukuchelewesheni kuingia Msikiti Mtakatifu. Basi amekujaalieni kabla ya kuingia kwenu mpate Ushindi karibuni.

28 Yeye ndiye Mwenyezi Mungu aliye mtuma Mtume wake na uwongozi ulio wazi, na Dini ya Kiislamu, ili itukuke juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa ni Shahidi wa hayo

29 Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Masahaba wake walio pamoja naye, ni wakali na wenye nguvu kwa makafiri, na wanarehemeana na kuoneana huruma wenyewe kwa wenyewe. Unawaona wakirukuu na kusujudu sana, wakiomba kwa hivyo thawabu kubwa kwa Mwenyezi Mungu, na radhi za kuenea. Alama yao ni unyenyekevu wao katika nyuso zao kutokana na kuathirika kwa Sala nyingi. Hiyo ndiyo sifa yao kubwa katika Taurati. Na sifa yao katika Injili ni kama mmea ulio chipua ukapata nguvu, ukageuka kutokana na udhaifu ukawa mgumu, ukasimama sawa sawa kwenye shina lake. Ukawafurahisha wakulima kwa nguvu zake. Basi Waumini ni hali kadhaalika, ili Mwenyezi Mungu awakasirisha makafiri kwa nguvu zao. Mwenyezi Mungu amewaahidi walio amini na wakatenda mema katika wao maghfira ya kuwafutia madhambi yao yote, na thawabu kubwa mno.

(Katika Injili ya Marko 4.26-28 imeandikwa: “Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi huzaa wenyewe; kwanza jani, tena suke, tena ngano pevu katika suke.” Katika Hesabu 16.22 ambacho ni sehemu ya Taurati kwa mujibu wa Biblia imeandikwa kuwa Musa na Haruni walisali kwa kusujudu. Humo inasemwa: “Nao wakapomoka kifudufudi, wakasema, Ee Mungu...” Na katika Injili ya Mathayo 26.39 inatajwa pia kuwa Yesu pia alisali kwa kusujudu: “Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifulu, akaomba...” Hivyo ndivyo wasalivyo Waislamu.)

Sura 49 - Al-H'ujuraat

Utangulizi

Imeanza Sura hii kwa kuwakataza Waumini kuhukumia kitu kabla Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawajaamrisha, na pia wasinyanyue sauti zao juu ya sauti ya Nabii s.a.w. Na imewasifu wale wanao teremsha sauti zao mbele yake. Na imewalaumu wanao kosa adabu wakampigia kelele Mtume s.a.w. nyuma ya vyumba, yaani naye yuko ndani nyumbani kwake. Kisha ikawaamrisha Waumini wahakikishe khabari za wapotovu na wachache wa Imani, na ikwaamrisha wenye madaraka nini la kutenda wanapo pigana makundi mawili ya Waumini wenyewe kwa wenyewe. Na imewakataza Waumini wasifanyiane kejeli wao kwa wao. Na imewakataza wakaazi wa majangwani kudai kuwa wana Imani kabla haijatua hiyo Imani katika nyoyo zao. Kisha Sura imebainisha ni nani hao Waumini wa kweli, na ikahitimishia mazungumzo kwa kukataza kumsimbulia Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kusilimu kwao. Na ikabainisha kwamba hakika aliye fanya hisani juu yao ni Mwenyezi Mungu kwa kuwaongoza kwenye Imani, ikiwa wao ni wasema kweli katika madai yao.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Enyi mlio amini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.¹
2. Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyo semezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui.²
3. Kwa hakika wanao teremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa uhamngu. Hao watakuwa na maghfira na ujira mkubwa.³
4. Hakika hao wanao kuita nawe uko nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili.⁴
5. Na lau wao wangeli ngojea mpaka uwatokee ingeli kuwa kheri kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira, Mwenye kurehemu.⁵

1 Enyi mlio amini! Msitangulie na kulikata jambo lolote la kidini na la kidunia bila ya kukuamrisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na jiwekeeni kinga ya nafsi zenu isikupateni adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kufuata sharia yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia baraabara yote mnao yasema, ni Mwenye kuyajua vilivyo mambo yote.

2 Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu juu ya sauti ya Nabii anapo sema na nyinyi mnasema. Wala msipambanisha sauti zenu na sauti yake, kama mnapo semezana nyinyi kwa nyinyi, kwa kuchelea visiharibike vitendo vyenu bila ya nyinyi wenyewe kutambua.

3 Hakika wanao teremsha sauti zao katika baraza ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kumtukuza yeye, hao peke yao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa uhamngu. Kwa wengineo si hivyo. Nao watapata msamaha mkubwa kufutiwa madhambi yao, na thawabu zilizo fika ukomo wa kufika kwake.

4 Hakika hao wanao kuita kwa makelele nawe uko vyumbani mwako wengi wao hawafahamu yanayo takikakana kukuhishimu na kukutukuza kwa makamo yako.

5 Na lau kuwa hao wangeli ngojea, kwa kukufanyia adabu, mpaka ukatoka, bila ya shaka ingeli kuwa ni

6. Enyi mlio amini! Akikujieni mpotovu na khabari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kuto jua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyo yatenda.⁶
7. Na jueni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko nanyi. Lau angeli kut'iini katika mambo mengi, bila ya shaka mngeli taabika. Lakini Mwenyezi Mungu amekupendezeeni Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na amekufanyeni muuchukie ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walio ongoka,⁷
8. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na neema zake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima.⁸
9. Na ikiwa makundi mawili katika Waumini yanapigana, basi yapatanisheni. Na likiwa moja la hao linamdhulumu mwenzie, basi lipigeni linalo dhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu. Na likirudi basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao hukumu kwa haki.⁹
10. Hakika Waumini ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe.¹⁰
11. Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu.¹¹
12. Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi

bora zaidi katika Dini yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mkubwa wa kusamehe, Mwenye rehema kunjufu.

6 Enyi mlio amini! Akikujieni mtu ambaye yuko nje ya sharia ya Mwenyezi Mungu akakupeni khabari yoyote, basi chungueni mjue ukweli wake, kwa kuchelea msije mkawaletea watu madhara, kwa kutojua hali yao. Hapo tena baada ya kwisha dhiri kuwa hawana makosa mkaingia katika majuto ya daima, mkatamani yasingeli kuwa.

7 Na jueni, enyi Waumini, kwamba Mtume yuko nanyi. Basi mkadirieni kama anavyo stahiki kadiri yake, na msadikini. Lau yeye angeli wafuata walio wachache wa Imani kati yenu katika mambo mengi, basi hapana shaka mngeli ingia katika mashaka na hilaki. Lakini Mwenyezi Mungu amewapendezesha Imani wale walio kamilika katika nyinyi, na akaipamba katika nyoyo zenu. Basi jilindeni na kujipamba na yasiyo takikana. Na amekufanyeni mchukie kukufuru neema za Mwenyezi Mungu, na kutokana na sharia zake, na kwenda kinyume na amri zake. Hao tu, peke yao, ndio wanao ijua njia ya uwongofu na wameishikilia. Na hiyo ni fadhila tukufu na neema kubwa ya Mwenyezi Mungu juu yao. Na Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu kwa ujuzi wake, ni Mwenye hikima ya kupita mpaka katika kuendesha kila jambo.

8 Tazama tanbihi ya 7.

9 Na ikiwa makundi mawili ya Waumini yanapigana, basi enyi Waumini, yapatanisheni. Ikiwa moja ndilo linalishambulia la pili, na likakataa kupatanishwa, basi lipigeni hilo linalo shambulia, mpaka lirejee kwenye hukumu ya Mwenyezi Mungu. Likirejea basi wapatanisheni kwa insafu. Na fanyeni uadilifu baina ya watu wote katika kila jambo. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wenye kufanya uadilifu.

10 Hakika wote wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni ndugu, Imani imezifanya nyoyo zao pamoja. Basi patanisheni baina ya ndugu zenu kwa kufuata udugu wa Imani. Na jiwakeeni nafsi zenu kinga cha kuinga adhabu ya Mwenyezi Mungu, kwa kufuata amri yake, na kuepuka anayo yakataza, na huku mkitaraji Mwenyezi Mungu akurehemuni kwa uchungu wenu.

11 Enyi mlio amini! Wanaume katika nyinyi wasiwadharau wanaume wenginewe, huenda hao mbele ya Mwenyezi Mungu wakawa bora kuliko wao. Wala wanawake Waumini wasiwadharau wanawake wenzao, huenda pengine wakawa hao ni bora kwa Mwenyezi Mungu kuliko wao. Wala msifanye kuaibishana nyinyi kwa nyinyi, wala mtu asimwite mwenzie kwa jina la kumuudhi. Ni uovu mno kwa Waumini kutajwa kwa upotovu baada ya kwisha sifika kwa Imani. Na wasio rudi wakaacha waliyo katizwa, basi hao peke yao ndio walio jidhulumu nafsi zao na wakawadhulumu wengineo.

anaye penda kuila nyama ya nduguye aliye kufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.¹²

13. Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.¹³

14. Mabedui wamesema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani Imani haijaingia katika nyoyo zenu. Na mkimt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hatakupunguzieni chochote katika vitendo vyenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.¹⁴

15. Hakika Waumini ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wakweli.¹⁵

16. Sema: Ati ndio mnamfundisha Mwenyezi Mungu Dini yenu, na hali Mwenyezi Mungu anayajua ya katika mbingu na ardhi, na Mwenyezi Mungu anajua kila kitu?¹⁶

17. Wanakusimbulia kuwa wamesilimu! Sema: Msinisimbulie kwa kusilimu kwenu. Bali Mwenyezi Mungu ndiye aliye kufanyieni hisani kwa kukuongoeni kwenye Imani, ikiwa nyinyi ni wakweli.¹⁷

18. Hakika Mwenyezi Mungu anajua siri za mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu anayaona myatendayo.¹⁸

12 Enyi mlio amini, jitengeni mbali na wingi wa kudhania dhana mbovu kwa watu wa kheri. Kwani hakika baadhi ya dhana ni dhambi zinazo stahiki adhabu. Wala msiwe mkitafta aibu za Waislamu. Wala msisengenyane, yaani kumsema mtu nyuma yake kwa jambo linalo muudhi. Hebu yupo yeyote kati yenu anaye penda kula nyama ya nduguye aliye kufa? Bila ya shaka hayo yanakuchukizeni! Basi ichukieni pia tabia ya kusengenyana na kusemana, kwani haya nayo ni mfano wa hayo. Na zikingeni nafsi zenu na adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kufuata amri zake, na kuyaepuka ayakatazayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkubwa wa kukubali toba ya wenye kutubia, Mwenye rehema kunjufu kwa walimwengu wote.

13 Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni nyinyi sawa sawa kutokana na asli moja, ya Adamu na Hawa. Na tukakufanyeni mkawa wengi kwa mataifa makubwa na makabila mengi, ili kutimie kujuana na kuawiniana baina yenu, sio kubaguana. Na hakika mwenye cheo cha juu miongoni mwenu kwa Mwenyezi Mungu duniani na Akhera ni yule anaye mcha Yeye zaidi. Hakika Mwenyezi Mungu amevizunguka vitu vyote kwa kuvijua, ni Mwenye khabari za dogo na kubwa la kila jambo.

14 Wakaazi wa majangwani wamesema kwa ndimi zao: Tumeamini. Ewe Muhammad! Waambie: Bado hamjaamini; kwa sababu nyoyo zenu bado hazijasadiki hayo mnayo yatamka. Lakini nyinyi semeni: Tumefuata dhaahiri ya Ujumbe wako. Bado Imani haijaingia katika nyoyo zenu. Na mkimt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kweli, hato kunyimeni hata chembe katika malipo ya vitendo vyenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkubwa wa kuwasamehe waja wake, ni Mwenye rehema kunjufu kwa kila kitu.

15 Hakika Waumini wa kweli ni wale ambao wanamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kisha hapana shaka yoyote inayo ingia katika nyoyo zao kwa hayo wanayo yaamini; tena wakapigana Jihadi kwa kutoa mali yao na roho zao katika njia ya ut'iifu wa Mwenyezi Mungu. Hao peke yao ndio walio wakweli katika Imani yao.

16 Ewe Muhammad! Waambie kwa kuwakanusha ile kauli yao kuwa wameamini: Ndio hivyo ati mnampa khabari Mwenyezi Mungu kuwa nyoyo zenu zimesadiki? Na Mwenyezi Mungu peke yake anajua kila kiliomo katika mbingu na katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu amevizunguka vitu vyote kwa ujuzi wake.

17 Wanaona kuwa kusilimu kwao ni kukuunga mkono wewe, Muhammad, na hivyo inastahiki wewe uwashukuru. Sema: Msinisimbulie kusilimu kwenu; kwani kheri yake mnaipata nyinyi. Bali ni Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye kufanyieni ihsani kwa kukuongoeni kwenye Imani, ikiwa nyinyi ni wakweli katika hayo madai yenu.

18. Hakika Mwenyezi Mungu anajua kila lilio fichikana katika mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuona vyema yote myatendayo.

Sura 50 - Qaaf

Utangulizi

Mwanzo wake Sura hii inasimulia kuthibiti Utume wa Muhammad s.a.w. na wanavyo kanya makafiri kuja Mtume kati yao, na kuona muhali kufufuliwa baada ya kwisha geuka udongo. Na ikaeleza Ishara za uumbaji zinazo onyesha dalili ya kwamba Mwenyezi Mungu hashindwi kuwafufua watu baada ya kufa kwao, na hali Yeye ndiye aliye waumba hapo kwanza, na anajua yanayo wapitikia katika nafsi zao. Na Yeye anavisajili vitendo vyao na maneno yao katika Daftari lenye kuhifadhi hata dogo. Na Sura imebainisha kwamba majaribio ya makafiri Siku ya Kiyama kutaka kuukataa ukafiri walio kuwa nao duniani, ati kwa kusingizia walikuwa ni wafwasi tu wa Mashetani hayatawaletea nafuu yoyote. Kwani mwisho wa mjadala wao ni kutumbukizwa wote katika Moto, na huku Mwenyezi Mungu anawafadhili Waumini kwa kuwapa neema za milele katika Pepo. Kisha Sura inamalizikia masimulizi yake kwa kumuamrisha Mtume s.a.w. avumilie maudhi ya makafiri ambao hawakuzingatia yaliyo wapata walio kadhibisha katika kaumu zilizo kuwa kabla yao, na kumwelekeza Mtume s.a.w. athibiti juu ya ibada ya Mwenyezi Mungu, na kutilia mkazo hili jambo la kufufuliwa, na kumliwaza Mtume s.a.w. kwa kuwa yeye ni mwenye kuwakumbusha Waumini, wala si mtawala wa makafiri.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Qaaf. Naapa kwa Qur'ani tukufu!¹
2. Bali wanastaajabu kwamba amewafikia mwonyaji kutoka miongoni mwao, na wakasema makafiri: Hili ni jambo la ajabu!²
3. Ati tukifa na tukawa udongo? Kurejea huko kuko mbali!³
4. Hakika Sisi tunajua kiasi cha kila kinacho punguzwa na ardhi kutokana nao. Na kwetu kipo Kitabu kinacho hifadhi yote.⁴
5. Lakini waliikanusha Haki ilipo waja; kwa hivyo wamo katika mambo ya mkorogo.⁵
6. Je! Hawaangalii mbingu zilizo juu yao! Vipi tulivyo zijenga, na tukazipamba. Wala

1 Qaaf. Hii ni harufi katika harufi za alifbete iliyo fungulia Sura hii kama ilivyo ada ya Qur'ani katika kufungulia Sura kadhaa wa kadhaa kwa harufi kama hii, ili kuwakabili makafiri kama wanaweza kuleta mfano wake, na pia kuwazindua watu wasikilize yanayo somwa. Ninaapa kwa Qur'ani yenye ubora, na utukufu, na hishima kwamba hakika Sisi tumekutuma wewe, ewe Muhammad, ili uwaonye watu kwa hii. Na watu wa Makka hawakuamini, bali walistaajabu kutokea Mtume miongoni mwa jinsi yao akiwaonya kuwa watafufuliwa. Makafiri wakasema: Jambo hili hatulijui, na la ajabu!

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Ati baada ya kwisha kufa na tukawa udongo, tutafufuliwa tena? Huko kufufuliwa baada ya kufa ni marejeo yaliyo mbali, hayawi.

4 Sisi hakika tunajua vipi ardhi inavyo vimeza viwiliwili vyao baada ya kufa. Na Sisi tunacho Kitabu kinacho dhibiti na kuhifadhi kila kitu hata kidogo.

5 Wao hawayazingatii aliyo kuja nayo Mtume, bali walimkadhibisha mara tu bila ya kuzingatia na kufikiri. Basi wao wamo katika hali ya kubabaika, hawana utulivu.

hazina nyufa.⁶

7. Na ardhi tumeitandaza na tukaiwekea milima, na tukaiotesha mimea mizuri ya kila namna.⁷

8. Yawe haya ni kifumbua macho na ukumbusho kwa kila mja mwenye kuelekea.⁸

9. Na tumeteremsha kutoka mbinguni maji yaliyo barikiwa, na kwa hayo tukaotesha mabustani na nafaka za kuvunwa.⁹

10. Na mitende mirefu yenye makole yaliyo zaa kwa wingi,¹⁰

11. Ili iwe ni riziki kwa waja wangu. Na tukaifufua kwa maji nchi iliyo kuwa imekufa. Kama hivyo ndivyo utakavyo kuwa ufufuaji.¹¹

12. Kabla yao walikadhibisha kaumu ya Nuhu na wakaazi wa Rassi na Thamudi.¹²

13. Na A'di na Firauni na kaumu ya Lut'i.¹³

14. Na wakaazi wa Machakani, na watu wa Tubbaa'. Wote hao waliwakanusha Mitume, kwa hivyo onyo likathibitika juu yao.¹⁴

15. Kwani tulichoka kwa kuumba mara ya kwanza. Bali wao wamo katika shaka tu juu ya umbo jipya.¹⁵

16. Na hakika tumemuumba mtu, nasi tunajua yanayo mpitikia katika nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake.¹⁶

17. Wanapo pokea wapokeaji wawili, wanao kaa kuliani na kushotoni.¹⁷

18. Hatamki neno ila karibu yake yupo mwangalizi tayari.¹⁸

19. Na uchungu wa kutoka roho utamjia kwa haki. Hayo ndiyo uliyo kuwa ukiyakimbia.¹⁹

6 Wameghafilika hata hawaitazami mbingu ilivyo nyanyuliwa juu yao bila ya nguzo? Vipi tumetengeneza ujenzi wake, na tukaipamba kwa nyota, na haina nyufa za kuitia kombo! (*Tazama Maelezo 50:6*)

7 Na ardhi tumeikunjua na tukaisimamisha milima iliyo kaa imara na kuthibiti kwenda chini. Na tukaijaalia kumea kila namna ya mimea mizuri ya kuwafurahisha watazamao. (*Tazama Maelezo 50:7*)

8 Tumejaalia hayo aone na akumbuke kila mja mwenye kurejea kwa Mola wake Mlezi, akafikiri Ishara za uwezo wake.

9 Na kutoka mbinguni tukateremsha maji yenye kheri nyingi na baraka, na kwa hayo tukaotesha mabustani yenye miti, na mauwa, na matunda, na tukatoa kwa hayo nafaka za makulima ya kuvunwa.

10 Na mitende mirefu mirefu, yenye makole ya tende yaliyo pandana kwa wingi

11 Tumeotesha hiyo ili iwe ni riziki kwa waja wetu, na tukaihuisha kwa maji ardhi iliyo kauka mimea yake. Hali kadhaalika ndivyo kufufuliwa wafu kutoka makaburini.

12 Kabla ya hawa, kaumu nyingi ziliwakadhibisha Mitume- kaumu ya Nuhu, na kaumu nyengine iliyo kuwa ikiitwa "Watu wa Rassi", na wa Thamudi, na wa A'di, na wa Firauni, na kaumu Lut'i, na kaumu iliyo kuwa maarufu kwa jina la "Watu wa Machakani", na kaumu ya Tubbaa' - wote hao waliwakadhibisha Mitume wao. Kwa hivyo wakastahiki maangamizo niliyo waahidi.

13 Tazama tanbihi ya 12.

14 Tazama tanbihi ya 12.

15 Kwani kutaka kwetu kulipungua, au uwezo wetu ulitetereka, hata tukashindwa kwa kule kuumba kwa mara ya kwanza, tusiweze tena kuwarejeza? Hasha! Hatukushindwa, nao wanatambua hayo. Bali wao wana shaka tu na wanadanganyikiwa na huku kuumbwa kupya baada ya kufa.

16 Ninaapa: Bila ya shaka tumemuumba mtu, na Sisi tunajua hata anayo semezwa na nafsi yake. Na Sisi kwa kuzijua hali zake zote, ni karibu kuliko mshipa wake wa damu ulioko shingoni mwake. Na hicho ndicho kitu kilicho karibu mno naye.

17 Watakapo kutana Malaika wawili walinzi, mmoja anakaa kuliani, na mwingine anakaa upande wa kushoto, wakiviandika vitendo vyake.

18 Halimtoki neno ila yuko karibu naye Malaika tayari kuandika neno lake.

19 Na yatapo kuja machungu ya kukata roho, kwa haki isiyo na shaka ndani yake, hilo ni jambo la kweli ulilo kuwa ukilikimbia.

20. Na litapulizwa baragumu. Hiyo ndiyo Siku ya Miadi.²⁰
21. Na kila nafsi itakuja na pamoja nayo mchungaji na shahidi.²¹
22. (Aambiwe): Kwa hakika ulikuwa umeghafilika na haya; basi leo tumekuondolea pazia lako, na kwa hivyo kuona kwako leo ni kukali.²²
23. Na mwenzake atasema: Huyu niliye naye mimi kesha tayarishwa.²³
24. Mtupeni katika Jahannamu kila kafiri mwenye inda,²⁴
25. Akatazaye kheri, arukaye mipaka, mwenye kutia shaka,²⁵
26. Aliye weka mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu. Basi mtupeni katika adhabu kali.²⁶
27. Mwenzake aseme: Ee Mola wetu Mlezi! Sikumpoteza mimi, bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotovu wa mbali.²⁷
28. (Mwenyezi Mungu) aseme: Msigombane mbele yangu. Nilikuleteeni mbele onyo langu.²⁸
29. Mbele yangu haibadilishwi kauli, wala Mimi siwadhulumu waja wangu.²⁹
30. Siku tutapo iambia Jahannamu: Je! Umejaa? Nayo itasema: Je! Kuna ziada?³⁰
31. Na Pepo italetwa karibu kwa ajili ya wachamngu, haitakuwa mbali.³¹
32. Haya ndiyo mnayo ahidiwa kwa kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu na akajilinda.³²
33. Mwenye kumwogopa Mwingi wa Rehema hali kuwa hamwoni, na akaja kwa moyo ulio elekea-³³

20 Na baragumu litapulizwa kwa mpulizo wa kuwafufua watu. Kupulizwa huko kutakuwa siku hiyo ya kuteremka adhabu waliyo ahidiwa.

21 Na kila nafsi njema na mbaya, itakuja na pamoja nayo wa kuichunga kuipeleka kwenye mkusanyo, na wenye kuwatolea ushahidi wa vitendo vyao.

22 Wataambiwa, kumtisha huyo mwenye kukadhibisha: Hakika wewe huko duniani ulikuwa umeghafilika kabisa na haya unayo sononeka nayo hivi sasa. Basi Sisi tumekuondolea pazia lililo kuwa likikuziua usiyaone mambo ya Akhera. Basi jicho lako hii leo linaona kwa nguvu.

23 Na Shetani wake aliye kuwa mwongozi wake duniani, atasema: Kafiri huyu alioko kwangu yuko tayari kuingia Jahannamu kwa kupotezwa nami.

24 Malaika wawili wataambiwa: Watieni katika Jahannamu kila aliye pita mipaka kwa ukafiri, na aliye pita mipaka kwa inadi, na akaacha kuifuata Haki, na akapita mipaka kuziua kheri, mwenye kudhulumu akaipindukia Haki, mwenye kumtilia shaka Mwenyezi Mungu Mtukufu na aliyo yateremsha.

25 Tazama tanbihi ya 24.

26 Aliye mfanya mungu mwengine wa kumuabudu pamoja na Mwenyezi Mungu. Basi mtupeni huyo katika adhabu yenye mwisho wa ukali.

27 Shetani atasema kumrudi yule kafiri: Ewe Mola wangu Mlezi! Mimi siye niliye mfanya awe mwenye kua'si, lakini yeye mwenyewe alikuwa katika upotovu wa mbali na haki. Na mimi nilimsaidia tu kwa kumpotoa.

28 Mwenyezi Mungu Mtukufu atawaambia makafiri na wenzi wao: Msigombane mbele yangu hapa pahala pa hisabu na malipo. Na Mimi nilikuleteeni mbele duniani onyo juu ya kukufuru kwenu kuukataa Ujumbe wangu niliyo utuma kwenu. Nanyi hamkuamini.

29 Hapana la kugeuza kauli ilioko kwangu na onyo langu kuwatia makafiri Motoni, wala Mimi si Mwenye kuwadhulumu waja. Kwani simuadhibu mja yeyote bila ya makosa.

30 Siku tutapo iambia Jahannamu kwa kuwatia kiwewe makafiri: Je! Umejaa? Nayo Jahannamu iseme kwa kuwaghadhibikia: Wapo wengine zaidi wa kuwaozeza katika hawa wenye kudhulumu?

31 Na Pepo iliyo pambwa italetwa karibu kwa ajili ya wenye kumcha Mola wao Mlezi, kwa kufuata amri zake na kuyaepuka makatazo yake, iletwe pahala pasipo kuwa mbali nao.

32 Haya ndiyo malipo ya kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu, aliye mwingi wa kuhifadhi sharia zake.

33 Mwenye kukhofu adhabu ya Mwenyezi Mungu ambaye rehema yake imeenea juu ya kila kitu, na Yeye

34. (Ataambiwa) ingieni kwa salama. Hiyo ndiyo siku ya daima dawamu.³⁴
35. Humo watapata wakitakacho, na kwetu yako ya ziada.³⁵
36. Na kaumu ngapi tuliziangamiza kabla yao walio kuwa na nguvu zaidi kuliko hawa! Nao walitanga tanga katika nchi nyingi. Je! Walipata pa kukimbilia?³⁶
37. Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia.³⁷
38. Na bila ya shaka Sisi tumeziumba mbingu na ardhi na vilio baina yao mnamo siku sita; na wala hayakutugusa machofu.³⁸
39. Basi vumilia kwa hayo wasemayo, na mtakase kwa kumsifu Mola wako Mlezi kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa.³⁹
40. Na katika usiku pia mtakase, na baada ya kusujudu.⁴⁰
41. Na sikiliza siku atapo nadi mwenye kunadi kutoka pahala karibu.⁴¹
42. Siku watakapo sikia ukelele wa haki. Hiyo ndiyo siku ya kufufuka.⁴²
43. Hakika Sisi tunahuisha na tunafisha, na kwetu Sisi ndio marejeo.⁴³
44. Siku itapo wapasukia ardhi mbio mbio! Mkusanyo huo kwetu ni mwepesi.⁴⁴
45. Sisi tunajua kabisa wayasemayo. Wala wewe si mwenye kuwatawalia kwa ujabari. Basi mkumbushe kwa Qur'ani anaye liogopa onyo.⁴⁵

haonekani, na akaja Akhera na moyo wa aliye kwisha rejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

34 Itasemwa kwa hishima yao: Ingieni Peponi kwa amani. Hiyo siku mtakapo ingia Peponi ndiyo siku ya kubakia milele isiyu na mwisho.

35 Hao wachamngu watapata kila wakitakacho huko Peponi. Na Sisi tunazo neema za kuzidi kuliko yanayo mpitikia mtu kuyawaza.

36 Na wengi tumekwisha wateketeza kabla ya hawa wanao kadhibisha katika mataifa yaliyo kwisha pita. Wao walikuwa na nguvu na madaraka zaidi kuliko hawa. Wakaizunguka miji wakishughulika kuchungua na kutafuta. Je! Walipata pa kukimbilia wasiangamizwe?

37 Hakika kwa waliyo tendewa hao wa kaumu zilizo kwisha pita ni mawaidha kwa mwenye moyo wa kufahamu hakika ya mambo, au akasikiliza uwongofu naye akili zake anazo.

38 Ninaapa: Hakika tumeziumba mbingu na ardhi na viumbe viliomo baina yao katika siku sita. Na hatukupata kuchoka. (*Tazama Maelezo 50:38*)

39 Ikiwa haya yamebainika, basi, ewe Mtume, yastahamilie hayo wayasemayo hao wanao kanusha, ya uwongo na uzushi kukhusu Utume wako. Nawe mtakasishe, Msabbih, Muumba wako na Mlezi wako na kila upungufu, ukimhimidi wakati wa alfajiri, na wakati wa alasiri, kwani ibada nyakati hizo ni jambo kuu. Na pia mtakasishe, Msabbih, katika saa za usiku, na baada ya Sala.

40 Tazama tanbihi ya 39.

41 Na sikiliza khabari ninazo kwambia katika hadithi za Kiyama kwani shani yake ni kubwa. Siku atapo nadi Malaika wa kunadi kutoka pahala pa karibu na hao wanao itwa. Siku watapo sikia mpulizo wa pili wa Haki, nao ni wa kufufuliwa watu. Hiyo ndiyo siku ya kutoka kwenye makaburi.

42 Tazama tanbihi ya 41.

43 Hakika Sisi, peke yetu, ndio tunao huisha viumbe vyote, na tunavifisha duniani. Na kwetu Sisi, peke yetu, ndio marejeo Akhera.

44 Siku itakapo wapasukilia ardhi, na watoke humo mbio mbio wakikimbilia mkutanoni. Hilo jambo kuu la kuwakusanya wote ni dogo na jepesi kwetu.

45 Sisi tunajua kuliko yeyote hayo wayasemayo ya uwongo juu yaliyo khusu Utume wako. Wala wewe hukutumwa uwalazimishe kwa unayo yataka. Ila wewe ni mwonyaji basi mkumbushe kwa Qur'ani Muumini mwenye kuiogopa adhabu yangu ili ukumbusho umfae.

Sura 51 - Adh-Dhaariyaat

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kiapo cha ukweli wa kufufuliwa na kutokea malipo. Kisha ikafuatisha kwa kiapo kingine juu ya ubabaishi wa wanao kanya katika maneno yao juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, na juu ya Qur'ani tukufu. Kisha ikaingia kuwaonya wanao kanya kuwa watapata mwisho muovu katika Akhera. Tena ikaeleza waliyo ahidiwa wachamngu katika malipo ya vitendo vyao vyema walivyo vitanguliza duniani. Kisha ikawazindua watu wazingatie Ishara za Mwenyezi Mungu katika kuumba kwake, na katika nafsi zao, na katika mambo ya ufundi wa ajabu na uzuri wa umbo alio uweka humo.

Na ikasimulia kisa cha Ibrahim na wageni wake Malaika, kisha ikaeleza hali za baadhi ya mataifa na maangamizo yaliyo wasibu kwa kuwakadhibisha Manabii wao. Kisha ikaashiria kwa jumla baadhi ya Ishara za uumbaji, na ikahimiza watu warejee kwa Mwenyezi Mungu, na wamuabudu Yeye peke yake, ambayo hayo ndio makusudi ya kuumbwa majini na watu. Na Sura imekhitimisha kwa kuwaonya wanao mkadhibisha Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. kuwa watapata adhabu iliyo kwisha wapata kaumu za kabla yao.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa pepo zinazo tawanya,¹
2. Na zinazo beba mizigo,²
3. Na zinazo kwenda kwa wepesi.³
4. Na zinazo gawanya kwa amri,⁴
5. Hakika mnayo ahidiwa bila ya shaka ni kweli,⁵
6. Na kwa hakika malipo bila ya shaka yatatokea.⁶
7. Naapa kwa mbingu zenye njia,⁷
8. Hakika nyinyi bila ya shaka mmo katika kauli inayo khitalifiana.⁸
9. Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa.⁹

1 Ninaapa kwa pepo zinazo timua mawingu, zikayasukuma kwa nguvu, huku zikibeba mizigo mizito ya maji, zikawa zinakwenda kwa wepesi kwa amri ya Mwenyezi Mungu, zikawa zinagawanya riziki kwa ampendaye Mwenyezi Mungu.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Tazama tanbihi ya 1.

5 Hakika hayo mnayo ahidiwa, nayo ya kufufuliwa na mengineyo, ni hakika ya kweli itakayo tokea, na kwamba kwa yakini malipo kwa vitendo vyenu yatakuwa tu hapana hivi wala hivi.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Ninaapa kwa mbingu zenye njia zilizo wekwa baraabara, kwamba nyinyi msemapo mnayo yasema ni maneno ya kugongana.

8 Tazama tanbihi ya 7.

9 Huacha kuamini hiyo ahadi ya kweli na malipo yatakayo kuwa huyo anaye acha, kwa sababu amekhiari kufuata pumbao la nafsi yake kuliko akili yake.

10. Wazushi wameangamizwa.¹⁰
11. Ambao wameghafilika katika ujinga.¹¹
12. Wanauliza: Ni lini hiyo siku ya malipo?¹²
13. Hiyo ni siku watakayo adhibiwa Motoni.¹³
14. Onjeni adhabu yenu! Haya ndiyo mliyo kuwa mkiyahimiza.¹⁴
15. Hakika wachamngu watakuwa katika Mabustani na chemchem.¹⁵
16. Wanapokea aliyo wapa Mola wao Mlezi. Kwa hakika hao walikuwa kabla ya haya wakifanya mema.¹⁶
17. Walikuwa wakilala kidogo tu usiku.¹⁷
18. Na kabla ya alfajiri wakiomba maghfira.¹⁸
19. Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiye omba.¹⁹
20. Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini.²⁰
21. Na pia katika nafsi zenu - Je! Hamwoni?²¹
22. Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyo ahidiwa.²²
23. Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, hakika haya ni kweli kama ilivyo kweli kuwa nyinyi mnasema.²³
24. Je! Imekufikia hadithi ya wageni wa Ibrahim wanao hishimiwa?²⁴
25. Walipo ingia kwake wakasema: Salama! Na yeye akasema: Salama! Nyinyi ni watu nisio kujueni.²⁵
26. Akenda kwa ahali yake na akaja na ndama aliye nona.²⁶
27. Akawakaribisha, akasema: Mbona hamli?²⁷
28. Akahisi kuwaogopa katika nafsi yake. Wakasema: Usiwe na khofu, nao

10 Wameteketea waongo wanao sema katika khabari za Kiyama kuwa ni mambo ya dhana na kukisia tu, ambao kwamba wamezamishwa katika ujinga, wameghafilika na dalili za yakini.

11 Tazama tanbihi ya 10.

12 Wanauliza kwa kejeli, kwa kuwa wanaona hayawi hayo: Lini itakuwa hiyo siku ya malipo?

13 Siku watapo simamishwa Motoni wakichomwa!

14 Wataambiwa: Onjeni adhabu yenu hii ambayo duniani mlikuwa mkihimiza iwe.

15 Hakika walio mt'ii Mwenyezi Mungu na wakamkhofu watakuwa wananeemeka katika Mabustani na chemchem za Peponi ambazo haziwezi kusifika hakika yake.

16 Wakipokea thawabu na takrima wanazo pewa na Mola wao Mlezi. Hakika hao kabla ya hapo walikuwa duniani ni wenye kufanya mambo mazuri kwa kutimiza waliyo takiwa wayafanye.

17 Walikuwa kulala kwao usiku ni kuchache, na wakikisha sana kwa ibada, na mwishoni mwa usiku walikuwa wakiomba maghfira.

18 Tazama tanbihi ya 17.

19 Na katika mali yao wakiweka fungu maalumu lilio thibiti kwa ajili ya wenye haja, wanao omba na wanao jizulia kuomba kwa kujiteta.

20 Na katika ardhi zipo dalili nyingi zilizo wazi zinazo pelekea yakini, kwa mwenye kuitafuta njia.

21 Na hali kadhaalika katika nafsi zenu zipo Ishara zilizo wazi. Je! Mmeghafilika nazo, hamzioni.

22 Na katika mbingu ipo amri ya riziki zenu na kukadiriwa mnayo ahidiwa.

23 Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mbingu na ardhi kwamba hakika yote hayo mnayo yakanya kuwa, yaani kufufuliwa, kulipwa, kuadhibiwa wanao kadhibisha, na kuwalipa thawabu wachamngu, yote hayo bila ya shaka ni ya kweli thaabiti kama hivyo kusema kwenu ambako hamna shaka nako kuwa mnasema.

24 Unakijua kisa cha Malaika, wageni wa hishima wa Ibrahim? Pale walipo ingia kwake na wakamtolea Salamu, na yeye akawajibu kwa Salamu, na kuwambia kuwa ni watu asio wajua.

25 Tazama tanbihi ya 24.

26 Akenda kwa mkewe naye ana khofu, akaja na ndama aliye nona. Akawakaribisha, nao hawakula. Akasema kwa kuto wajua hakika yao: Mbona hamli?

27 Tazama tanbihi ya 26.

wakambashiria kupata kijana mwenye ilimu.²⁸

29. Ndipo mkewe akawaelekea, na huku anasema na akijipiga usoni kwa mastaajabu, na kusema: Mimi ni kikongwe na tasa!²⁹

30. Wakasema: Ndivyo vivyo hivyo alivyo sema Mola wako Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye hikima na Mwenye kujua.³⁰

31. AKASEMA: Basi ujumbe wenu ni nini, enyi mlilo tumwa?³¹

32. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwa watu wakosefu,³²

33. Tuwatupie mawe ya udongo,³³

34. Yaliyo tiwa alama kutoka kwa Mola wako Mlezi kwa ajili ya wanao pindukia mipaka.³⁴

35. Kwa hivyo tutawatoa katika hao wale walio amini.³⁵

36. Lakini hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu!³⁶

37. Na tukaacha humo Ishara kwa ajili ya wanao iogopa adhabu chungu.³⁷

38. Na katika khabari za Musa, tulipo mtuma kwa Firauni na hoja wazi.³⁸

39. Lakini alipuza kwa sababu ya nguvu zake na akasema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu!³⁹

40. Basi tukamkamata yeye na majeshi yake na tukawatupa baharini, na yeye ndiye wa kulaumiwa.⁴⁰

41. Na katika khabari za A'di tulipo wapelekea upepo wa kukata uzazi.⁴¹

42. Haukuacha chochote ulicho kifikia ila ulikifanya kama kilio nyambuka.⁴²

43. Na katika khabari za Thamudi walipo ambiwa: Jifurahisheni kwa muda mdogo tu.⁴³

28 Akahisi katika nafsi yake khofu kuwaogopa. Wakasema: Usiogope. Na wakampa bishara kuwa atapata mwana mwenye ilimu nzuri.

29 Akatokea mkewe akipiga kelele alipo isikia ile bishara, akijipiga uso wake kwa mkono wake, kwa kuona muhali hayo na kustaajabu, na akasema: Mimi ni kizee, na tasa. Itakuwaje nizae?

30 Wakasema: Hivyo ndivyo alivyo kwisha hukumu Mola wako Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye hikima katika kila anayo hukumu, ni Mwenye ujuzi ambaye hapana linalo fichikana kwake lolote.

31 Ibrahim akasema: Mna kazi gani tena baada ya khabari hii nzuri, enyi wajumbe?

32 Wakasema: Kwa hakika sisi tumetumwa kwa kaumu iliyo pita kiasi katika uasi, tuwatupie mawe ya udongo, ambayo hapana anaye yajua yalivyo ila Mwenyezi Mungu. Mawe hayo ni makhsusi na maalumu kwa Mola wako Mlezi kwa ajili ya wanao pindukia mipaka katika mambo machafu.

33 Tazama tanbihi ya 32.

34 Tazama tanbihi ya 32.

35 Basi tukahukumu tuwatoea kwenye mji huo walio amini. Lakini hatukukuta ila nyumba moja tu ndiye ya Waislamu.

36 Tazama tanbihi ya 35.

37 Na katika mji huo tumeacha alama ya maangamizo ya watu wake, ili wapate kuzingatia wanayo ikhofu adhabu chungu.

38 Na katika kisa cha Musa yapo mawaidha. Tulipo mtuma kwa Firauni, na tukatilia nguvu kwa kumpa ushahidi ulio wazi.

39 Firauni akapuza kumuamini Musa kwa kutegemea ati nguvu zake. Akasema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu!

40 Tukamchukua yeye na hao anao jitapia kwao, tukawatumbukiza baharini, naye ni mwenye kuyatenda hayo ya ukafiri na inda anayo laumiwa kwayo.

41 Na katika kisa cha A'di yamo mawaidha pia. Tulipo wapelekea upepo usio kuwa na kheri yoyote.

42 Upepo huo haupiti kwa kitu chochote ila hukia kama fupa lililo nyambuka.

43 Na katika kisa cha Thamudi ipo Ishara. Walipo ambiwa: Stareheni katika majumba yenu kwa muda maalumu. Wakajivuna na wakatakabari wasifuata amri ya Mola wao Mlezi. Basi radi ikawaangamiza nao

44. Wakaasi amri ya Mola wao Mlezi. Basi uliwanyakua moto wa radi nao wanaona.⁴⁴
45. Basi hawakuweza kusimama wala hawakuwa wenye kujitetea.⁴⁵
46. Na kaumu ya Nuhu hapo mbele. Hakika hao walikuwa watu wapotovu.⁴⁶
47. Na mbingu tumezifanya kwa nguvu na uwezo na hakika Sisi bila ya shaka ndio twenye uwezo wa kuzitanua.⁴⁷
48. Na ardhi tumeitandaza; basi watandazaji wazuri namna gani Sisi!⁴⁸
49. Na katika kila kitu tumeumba kwa jozi ili mzingatie.⁴⁹
50. Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu, hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae kwake.⁵⁰
51. Wala msifanye kuwa kuna mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu. Hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae kwake.⁵¹
52. Basi ndio hivyo hivyo, hakuwajia kabla yao Mtume ila walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu.⁵²
53. Je! Wameambizana kwa haya? Bali hawa ni watu waasi.⁵³
54. Basi waachilie mbali, nawe hulaumiwi.⁵⁴
55. Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa Waumini.⁵⁵
56. Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.⁵⁶
57. Na sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishie.⁵⁷
58. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, Madhubuti.⁵⁸
59. Hakika walio dhulumu wana fungu lao la adhabu kama fungu la wenzao. Basi wasinihimize.⁵⁹

wanaiona kwa macho yao inavyo tokea.

44 Tazama tanbihi ya 43.

45 Basi hawakuweza kuinuka. Wala hawakuweza kujipigania kuijikinga na adhabu.

46 Na kaumu ya Nuhu tulihihili kabla ya hawa. Hakika hao walikuwa watu walio toka nje ya ut'iifu wa Mwenyezi Mungu.

47 Na mbingu tumeipanga kwa nguvu, na bila ya shaka Sisi ni waweza zaidi ya hayo. Na ardhi tumeikunjua, na Sisi ni wenye kuitengeza vizuri kama kitanda. (*Tazama Maelezo 51:47*)

48 Tazama tanbihi ya 47.

49 Na kila kitu tumekiumba namna mbili, yaani kwa jozi, ili mpate kukumbuka muuamini uwezo wetu.

50 Basi fanyeni haraka kuendea kwenye ut'iifu wa Mwenyezi Mungu. Wala msifanye mungu mwengine kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu. Hakika mimi nimekujieni kwa amri ya Mwenyezi Mungu kukuonyeni kwa uwazi matokeo ya ushirikina.

51 Tazama tanbihi ya 50.

52 Hivyo ndivyo ilivyo kuwa hali ya mataifa yote kwa Mitume wao. Hakuja Mtume kwa watu wa kabla ya kaumu yako ila walimwita: Mchawi au mwendawazimu.

53 Je! Mmeusiana, mmeambizana, nyinyi kwa nyinyi kusema hivyo ndio maana mnalirejea hilo kwa hilo? Bali hao ni watu walio pindukia mipaka, ndio wakawafikiana katika kuwashutumu Mitume!

54 Basi wapuuzilie mbali hawa wenye inda! Wewe hulaumiki usipo wajibu kitu.

55 Wewe dumisha kukumbusha, kwani ukumbusho huwazidisha Waumini kufumbua macho na kuwa na nguvu za yakini.

56 Wala sikuwaumba majini na watu kwa jambo la kuniletea Mimi manufaa, bali ili waniabudu, na kuniabudu Mimi ni manufaa kwao.

57 Sitaki kwao riziki, kwani Mimi si mhitaji kwa walimwengu wote; wala sitaki wanilishie, kwani Mimi ndiye ninaye lisha, wala silishwi.

58 Hakika Mwenyezi Mungu peke yake, ndiye mdhamini wa kuwapa riziki waja wake, na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Aliye imara, hashindikiki.

59 Hakika hao walio jidhulumu nafsi zao kwa ukafiri na kukanusha wana fungu lao la adhabu mfano wa fungu la wenzao katika kaumu zilizo kwisha pita. Basi wasifanye haraka kuhimiza adhabu ishuke kabla

60. Ole wao walio ikanusha siku yao waliyo ahidiwa.⁶⁰

ya wakati wake.

60 Basi maangamio yatawapata wenye kuikataa siku yao waliyo ahidiwa, kwa sababu ya shida na vitisho viliomo katika siku hiyo.

Sura 52 - Att'ur

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kiapo cha watano katika bora wa viumbe kuwa adhabu itawateremkia hao wanao kanusha. Kisha ikafikia kusimulia kuwateremkia hiyo adhabu, na namna zake mbali mbali siku ya kufufuliwa na kulipwa. Na ikaingia kutaja mazungumzo juu ya neema za wachamngu na watakayo stareheshwa nayo katika Mabustani ya milele, na namna ya ukarimu watacao upata, na kisha yatakavyo tua macho yao kwa kuwa dhuriya zao watavyo wafuata, na kunyanyuliwa vyeo vyao wawafikie wao. Na baada ya hayo Sura inamuamrisha Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. adumishe kukumbusha bila ya kujali wanayo mzulia makafiri kumpinga yeye, au kushughulika na wayasemayo juu ya Qur'ani tukufu, kwa vile inavyo onyesha kuwa wameshindwa kuleta maneno mfano wa Qur'ani.

Sura hii pia imekashifu maoni yao makafiri ya ufisadi ya kutangaza upotovu wao, na uovu wa kupima kwao. Kisha ikakhitimishia kwa kumuelekea Nabii s.a.w. na kumwambia awaachilie mbali mpaka watakapo ikuta siku yao watapo situshwa, naye akaamrisha aistahamilie hukumu ya Mola wake Mlezi ya kuwapa muhula hao, kwani hayo hayatamdhuru kitu yeye kwa sababu yumo katika uhifadhi wa Mola wake Mlezi na ulinzi wake. Kadhaalika imemtaka amtakase Mwenyezi Mungu na katika nyakati zote, na katika kila msimamo atakao kuwamo kwa jambo lolote, na usiku zinapo tua nyota

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa mlima wa T'ur,¹
2. Na Kitabu kilicho andikwa²
3. Katika ngozi iliyo kunjuliwa,³
4. Na kwa Nyumba iliyo jengwa,⁴
5. Na kwa dari iliyo nyanyuliwa,⁵
6. Na kwa bahari iliyo jazwa,⁶
7. Hakika adhabu ya Mola wako Mlezi hapana shaka itatokea.⁷

1 Ninaapa kwa mlima wa T'ur ulioko katika Sinai. Kwenye mlima huo ndio Nabii Musa a.s. alisemezwa. Na naapa kwa Kitabu kilicho teremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu kilicho andikwa katika kurasa zilio nyepesi kuzisoma, na kwa Nyumba iliyo jengwa kwa sababu ya wenye kuizunguka kwa ibada na wenye kusimama na kurukuu na kusujudu kwa Sala, na naapa kwa mbingu iliyo nyanyuliwa bila ya nguzo, na bahari iliyo jaa.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Tazama tanbihi ya 1.

5 Tazama tanbihi ya 1

6 Tazama tanbihi ya 1.

7 Hakika adhabu ya Mola wako Mlezi waliyo ahidiwa makafiri bila ya shaka itawateremkia hapana hivi wala hivi. Hapana wa kuizuia isiwafikilie.

8. Hapana wa kuizuia.⁸
9. Siku zitakapo tikisika mbingu kwa mtikiso,⁹
10. Na milima iwe inakwenda kwa mwendo mkubwa.¹⁰
11. Basi ole wao siku hiyo hao wanao kadhibisha,¹¹
12. Ambao wanacheza katika mambo ya upuuzi.¹²
13. Siku watapo sukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu,¹³
14. (Waambiwe): Huu ndio ule Moto mlio kuwa mkiukanusha!¹⁴
15. Je! Huu ni uchawi, au hamwoni tu?¹⁵
16. Uingieni, mkistahamili au msistahamili - ni mamoja kwenu. Hakika mnalipwa kwa mliyo kuwa mkiyatenda.¹⁶
17. Hakika wachamngu watakuwa katika Mabustani na neema,¹⁷
18. Wakifurahi kwa yale aliyo wapa Mola wao Mlezi. Na Mola wao Mlezi atawalinda na adhabu ya Motoni.¹⁸
19. Kuleni na kunyweni kwa raha kabisa kwa sababu ya mliyo kuwa mkiyatenda.¹⁹
20. Watakuwa wameegemea juu ya viti vya enzi vilivyo pangwa kwa safu. Na tutawaoza *mahuru-l-aini*.²⁰
21. Na walio amini na dhuriya zao wakawafuata kwa Imani tutawakutanisha nao dhuriya zao, na wala hatutawapunja hata kidogo katika vitendo vyao. Kila mtu lazima atapata alichu kichuma.²¹
22. Na tutawapa matunda, na nyama kama watavyo penda.²²
23. Watapeana humo bilauri zisio na vinywaji vya kuleta maneno ya upuuzi wala dhambi.²³

8 Tazama taanbhi ya 7

9 Siku mbingu itapo tikisika kwa mtikiso mkubwa, na milima itapo ng'oka kutoka hapo ilipo kwa kuonekana khasa.

10 Tazama tanbihi ya 9.

11 Maangamio makubwa yatawapata siku hiyo hao wanao kadhibisha Haki, ambao katika upotovu ndio mchezo wao wanapo chezea.

12 Tazama tanbihi ya 11.

13 Siku watakapo sukumwa kuingizwa Motoni kwa nguvu.

14 Wataambiwa: Huu ndio Moto mlio kuwa mkiukanusha duniani.

15 Je! Bado mnaendelea kuukanya. Huu Moto mnao uona ni uchawi, au hamwoni tu?

16 Uingieni, mpate kuonja vukuto lake. Mkivumilia shida zake, au mkitovumilia, kwenu ni mamoja. Hakika leo mtayakuta mliyo kuwa mkiyatenda duniani.

17 Hakika wachamngu watakuwa katika Mabustani yenye wasaa, hapana awezae kuyaeleza yalivyo, na neema kubwa kadhaalika.

18 Wakistarehe na neema alizo wapa Mola wao Mlezi, na Mola wao Mlezi akawalinda na adhabu ya Moto.

19 Wataambiwa: Kuleni chakula mpendacho, na kunyweni kwa raha, kuwa ni malipo ya vitendo mlivyo vitenda duniani.

20 Wakikaa nao wameegema juu ya makochi yaliyo pangwa kwa safu. Na tutawaoza wake weupe wenye macho ya vikombe wazuri.

21 Na walio amini, na wakastahiki vyeo vya juu, na vizazi vyao wakawafuata katika Imani, na wao hawajafikia daraja zile za baba zao, tutawakutanisha nao hao dhuriya zao, wapate kutulia nyoyo zao. Na wala hatuwapunguzii chochote katika thawabu za vitendo vyao. Wala wazazi hawatobeba chembe katika makosa ya dhuriya zao. Kwa sababu kila mtu amefungamana kwa rahani na vitendo vyake visio bebwa na mwenginewe.

22 Na tutawazidishia matunda mengi, na nyama kama waipendayo.

23 Huko Peponi watakuwa wakipeana kwa mapenzi bilauri zililo jaa vinywaji visio leta maneno yasiyo na

24. Iwe wanawapitia watumishi wao kama kwamba ni lulu zilizomo katika chaza.²⁴
25. Wataelekeana wakiulizana.²⁵
26. Waseme: Tulikuwa zamani pamoja na ahali zetu tukiogopa;²⁶
27. Basi Mwenyezi Mungu akatufanyia hisani na akatulinda na adhabu ya upepo wa Moto.²⁷
28. Hakika sisi zamani tulikuwa tukimwomba Yeye tu. Hakika Yeye ndiye Mwema Mwenye kurehemu.²⁸
29. Basi kumbusha! Kwani wewe, kwa neema ya Mola wako Mlezi, si kuhani wala mwendawazimu.²⁹
30. Au wanasema: Huyu ni mtunga mashairi, tunamtarajia kupatilizwa na dahari.³⁰
31. Sema: Tarajieni, na mimi pia ni pamoja nanyi katika kutarajia.³¹
32. Au hizo akili zao ndio zinawaamrisha haya, au wao basi ni watu majeuri tu?³²
33. Au ndio wanasema: Ameitunga hii! Bali basi tu hawaamini!³³
34. Basi nawalete masimulizi kama haya ikiwa wao wanasema kweli.³⁴
35. Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji?³⁵
36. Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana na yakini.³⁶
37. Au wanazo khazina za Mola wako Mlezi au wao ndio wenye madaraka?³⁷
38. Au wanazo ngazi za kusikilizia? Basi huyo msikilizaji wao na alete hoja ilio wazi!³⁸
39. Au Yeye Mwenyezi Mungu ana wasichana, na nyinyi ndio mna wavulana?³⁹

maana wala vitendo vya dhambi, yaani havilevi na kuondoa akili.

24 Na watakuwa wakiwapitia vijana walio wekwa kwa kuwatumikia, kwa weupe wao na usafi wao kama lulu iliomo ndani ya chaza.

25 Na watu wa Peponi watakabiliana wakiulizana wao kwa wao khabari za hayo mambo makuu wanayo yapata na sababu zake.

26 Kabla ya neema hizi sisi tulikuwa pamoja na ahali zetu tukiogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu akatufadhili kwa rehema yake, na akatukinga na adhabu ya Moto.

27 Tazama tanbihi ya 26.

28 Hakika sisi kabla ya haya tulikuwa duniani tukimuabudu Yeye tu. Yeye peke yake ndiye Mhisani Mkunjufu wa rehema.

29 Wewe endelea na kukumbusha kama unavyo fanya. Kwani wewe, kwa neema ya Mwenyezi Mungu aliyo kuneemesha kukupa Unabii na akili iliyo timia, si kuhani anaye toa khabari za ghaibu bila ya ilimu, wala si mwendawazimu unaye sema usiyo yasadiki.

30 Bali ati wanasema huyu ni mtunga mashairi, tunaye mngojea afikiwe na mauti! Waambie kwa kuwatisha: Ngojeeni, na mimi nami ni katika wanao ngojea mwisho wa hali yangu na hali yenu!

31 Tazama tanbihi ya 30.

32 Bali ndio akili zao zinawaamrisha waseme maneno hayo yanayo gongana. Kwani kohani na mtunga mashairi ni watu wenye fahamu na akili; na mwendawazimu hana akili. Lakini hawa ni watu walio pita mipaka katika inadi zao.

33 Bali ati wanasema: Muhammad ameizua hii Qur'ani! Bali hawa kwa ukaidi wao hawaamini tu.

34 Basi nawalete masimulizi kama haya ya Qur'ani, ikiwa wao ni wasema kweli kuwa Muhammad kaizua.

35 Kwani wao wameumbwa bila ya kuweko Muumbaji, au wao wamejiumba wenyewe, basi kwa hivyo ati ndio hawamtambui Muumbaji wa kumuabudu?

36 Kwani wao ndio walio ziumba mbingu na ardhi kwa uumbaji mzuri wa pekee wa namna hii? Bali wao hawana na yakini na lolote lilio mwajibikia Muumbaji. Na kwa hivyo ndio wanamshirikisha.

37 Kwani wao wanazo khazina za Mola wako Mlezi wanazo zisarifu watakavyo? Au wana nguvu za kutenda watakavyo, na kupanga mambo kama wapendavyo?

38 Bali wanacho kipandio cha kupandia mpaka mbinguni wakasikiliza anayo yahukumia Mwenyezi Mungu? Kama hivyo, basi nawamlete huyo mtu wao anaye sikiliza atoe hoja iliyo wazi kuthibitisha madai yake.

39 Ati Mwenyezi Mungu ndiye mwenye mabinti, kama mnavyo zua, na nyinyi ndio mna watoto wa kiume

40. Au wewe unawaomba ujira, na kwa hivyo ndio wanaelemewa na uzito wa gharama?⁴⁰
41. Au wanayo ilimu ya ghaibu, nao wameandika?⁴¹
42. Au wanataka kufanya vitimbi tu? Lakini hao walio kufuru ndio watakao tegeka.⁴²
43. Au wanae mungu asiye kuwa Mwenyezi Mungu? *Subhanallah!* Ametaksika Mwenyezi Mungu na hao wanao washirikisha naye.⁴³
44. Na hata wange ona pande linatoka mbinguni linaanguka wange sema: Ni mawingu yaliyo bebana.⁴⁴
45. Basi waache mpaka wakutane na siku yao watakapo hilikishwa.⁴⁵
46. Siku ambayo hila zao hazitawafaa hata kidogo, wala wao hawatanusuriwa.⁴⁶
47. Na hakika walio dhulumu watapata adhabu nyengine isiyo kuwa hii, lakini wengi wao hawajui.⁴⁷
48. Na ingojee hukumu ya Mola wako Mlezi. Kwani wewe hakika uko mbele ya macho yetu, na mtakase kwa kumsifu Mola wako Mlezi unapo simama,⁴⁸
49. Na usiku pia mtakase, na zinapo kuchwa nyota.⁴⁹

kama ndio mnavyo penda?

40 Kwani wewe unawaomba chochote kuwa ni ujira wa kuwafikishia Ujumbe wako, ndio wamethakilika na hizo gharama wakalalamika?

41 Bali kwani wao wanao ujuzi kujua mambo ya ghaibu, yaliyo fichikana, na hivyo wanaandika kutoka hayo wayatakayo?

42 Au wanataka kukufanyia vitimbi tu na kuuharibu Ujumbe wako? Basi hao walio kufuru ndio wanao stahiki kutumbukia katika vitimbi vyao.

43 Au wao wanae mungu wa kuabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu atakae walinda na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ametakasika na hayo wanayo mshirikisha naye!

44 Na wakiona kipande cha mbingu kinwaangukia kuwaadhibu wao husema, kwa inda tu: Ni mawingu yaliyo bebana!

45 Waache bila ya kuwajali mpaka watakapo ikuta siku yao watapo angamizwa.

46 Siku ambayo hila zao hazitawakinga hata na chembe ya adhabu, wala hawatapata wa kuwanusuru.

47 Na hakika hao walio dhulumu watapata adhabu mbali na hii waliyo teseka nayo hapa duniani, lakini wengi wao hawajui hayo.

48 . Wewe isubirie hukumu ya Mola wako Mlezi ya kuwapa muhula hao, na wewe kupata maudhi yao. Kwani hakika wewe umo katika hifadhi yetu na ulinzi wetu. Basi vitimbi vyao havitokudhuru wewe. Na mtakase kwa kumsifu Mola wako Mlezi unapo amka.

49 Na tafuta usiku usiku nafasi ya kumsabihi, yaani kumtakasa, Mwenyezi Mungu, na mtakase pia wakati zinapo kuchwa nyota, yaani alfajiri.

Sura 53 - Annajm

Utangulizi

Kiapo mwanzo wa Sura hii kinadhihirisha ukweli wa Mtume s.a.w. katika anayo yasimulia ya khabari za Wahyi (Ufunuo) na anayo yafikisha kutokana na huo ufunuo. Hakupoteza kitu katika hayo wala hakukosea. Na Mtume s.a.w. amesema kweli katika aliyo yazungumzia juu ya safari yake ya kwenda mbinguni, katika hayo yaliyo tokea ya Miiraji, jicho lake halikuhangaika wala halikuruka mpaka.

Kisha Sura inaingia kueleza uchache wa akili za makafiri kwenda kuabudu masanamu waliyo yaunda wenyewe kwa mikono yao, wakayaita majina yao wenyewe, kama walivyo waita Malaika kuwa ati ni wanawake, baada ya kumfanya Mwenyezi Mungu ana mabinti, na wao wenyewe wawe na watoto wa kiume.

Kisha Sura inamtaka Mtume s.a.w. awapuuze, na amwachilie mambo yao Mwenyezi Mungu Mwenye kumiliki na kuumba vyote viliomo mbinguni na kwenye ardhi. Na Yeye ndiye atakaye mlipa muovu kwa uovu wake, na mwema kwa wema wake. Naye ndiye Mjuzi kabisa wa yote yanayo pita kwa viumbe vyake na hali zao. Yakafwatia hayo kulaumiwa anaye kanya kuhisabiwa kila mtu kwa vitendo vyake, kama yalivyo kwisha pita kwa sharia zililo tangulia, na ikasimuliwa na Vitabu vya Musa na Ibrahim. Na Aya hizi zimethibitisha maana haya yaliyo elezwa katika uwezo na Ishara za Mwenyezi Mungu katika mataifa yaliyo kwisha tangulia.

Kisha Sura inakhitimisha kwa kuweka wazi kwamba Qur'ani ni onyo miongoni mwa maonyo walio onywa kwayo kaumu zilizo kwisha tangulia, ili wapate kutahadhari na Siku ya Kiyama ambayo imekaribia wakati wake. Na Sura inawalaumu makafiri wanao ikataa Qur'ani kwa kughafilika kwao huko, na wakawa wanacheka badala ya kulia na kuwaidhika kwa Qur'ani. Na ikawataka Waumini wamsujudie Mwenyezi Mungu aliye iteremsha na wamuabudu Yeye tu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa nyota inapo tua,¹
2. Mwenzenu huyu hakupotea, wala hakukosea.²
3. Wala hatamki kwa matamanio.³
4. Hayakuwa haya ila ni ufunuo ulio funuliwa,⁴
5. Amemfundisha aliye mwingi wa nguvu,⁵

1 Ninaapa kwa nyota inapo tua kwa kuchwa, ya kwamba Muhammad hakuiacha Njia iliyo sawa ya kufuata Haki, na wala hakupata kuitakidi upotovu.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Wala halitoki katika anayo yatamka ya Qur'ani kwa mapendo ya nafsi yake.

4 Hii Qur'ani anayo itamka si chochote ila ni Wahyi (Ufunuo) ulio toka kwa Mwenyezi Mungu anamfunulia yeye.

5 Aliye mfundisha ufunuo huu ni mwenye nguvu nyingi.

6. Mwenye kutua, akatulia,⁶
7. Naye yuko juu kabisa upeo wa macho.⁷
8. Kisha akakaribia na akateremka.⁸
9. Akawa ni kama baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi.⁹
10. Akamfunulia mja wake (Mwenyezi Mungu) alichu mfunulia.¹⁰
11. Moyo haukusema uwongo uliyo yaona.¹¹
12. Je! Mnabishana naye kwa aliyo yaona?¹²
13. Na akamwona mara nyingine,¹³
14. Penye Mkunazi wa mwisho.¹⁴
15. Karibu yake ndiyo ipo Bustani inayo kaliwa.¹⁵
16. Kilipo ufunika huo Mkunazi hicho kilicho ufunuika.¹⁶
17. Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka.¹⁷
18. Kwa yakini aliona katika Ishara kubwa kabisa za Mola wake Mlezi.¹⁸
19. Je! Mmemuona Lata na Uzza?¹⁹
20. Na Manaat, mwingine wa tatu?²⁰
21. Je! Nyinyi mnao wana wanaume na Yeye ndio awe na wanawake?²¹
22. Huo ni mgawanyo wa dhulma!²²
23. Hayo hayakuwa ila ni majina mliyo wapa nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuleta uthibitisho wowote juu ya hayo. Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi. Na kwa yakini uwongofu ulikwisha wafikia kutoka kwa Mola wao Mlezi.²³

6 Ambaye ametua akili zake na maoni yake, akasimama sawa sawa katika sura yake; naye yuko upande wa juu katika mbingu upeo wa macho wa mwenye kuangalia.

7 Tazama tanbihi ya 6.

8 Kisha Jibrili alimkaribia, na akazidi kukaribia, hata akawa ukaribu wake ni kiasi ya mipinde miwili, bali karibu kuliko hivyo.

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Jibrili akamfunulia mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, alichu mfunulia, nao ufunuo huo ni jambo lenye shani kubwa na athari ya mbali kabisa.

11 Moyo wa Muhammad haukukanya yale macho yake yaliyo yaona.

12 Hivyo nyinyi mnamkadhibisha Mtume wa Mwenyezi Mungu na mnabishana naye kwa aliyo yaona kwa macho yake.

13 Na bila ya shaka Muhammad alimwona Jibrili kwa sura yake mara nyengine, katika pahala pasipo juulikana ila na Mwenyezi Mungu tu, ambapo amepaita Sidratul muntahaa, "Mkunazi wa Mwisho". Na akasimulia kuwa hapo ndio ipo Jannatul Ma-awa, Bustani inayo kaliwa. Vikafunikwa na kuzibwa, kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu, visio weza kuelezwa. Jicho la Muhammad halikubabaika kwa aliyo yaona, na wala hakukiuka mpaka ya aliyo amrisha kwa kuona kwake huko.

14 Tazama tanbihi ya 13.

15 Tazama tanbihi ya 13.

16 Tazama tanbihi ya 13.

17 Tazama tanbihi ya 13.

18 Hakika ameona mengi katika Ishara za Mwenyezi Mungu na maajabu yake makubwa makubwa.

19 Je! Mmeyajua hayo, na mkayafikiri ya kina Lata na Uzza na Manata, huyo mwingine wa tatu, mlio wafanya kuwa ni miungu wa kuwaabudu?

20 Tazama tanbihi ya 19.

21 Mkagawa, nyinyi muwe na watoto wa kiume, na mkamfanyia Mwenyezi Mungu awe na watoto wa kike!

22 Huo basi ni ugawaji wa dhulma, mnamgawia Mwenyezi Mungu kile mnacho kichukia nyinyi wenyewe!

23 Hayo masanamu yenu si chochote ila ni majina tu yasiyo na maana yoyote ya kiungu. Mmeyatunga nyinyi na baba zenu kwa kufuata pumbao lenu la upotovu. Mwenyezi Mungu hakuteremsha nayo hoja

24. Ati mtu anakipata kila anacho kitamani?²⁴
25. Mwenyezi Mungu tu ndiye Mwenye dunia na Akhera.²⁵
26. Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipo kuwa baada ya Mwenyezi Mungu kutoa idhini kwa amtakaye na kumridhia.²⁶
27. Hakika wasio amini Akhera bila ya shaka wao ndio wanawaita Malaika kwa majina ya kike.²⁷
28. Nao hawana ujuzi wowote kwa hayo isipo kuwa wanafuata dhana tu. Na dhana haisaidii chochote mbele ya haki.²⁸
29. Basi mwachilie mbali anaye upa kisogo ukumbusho wetu, na wala hataki ila maisha ya dunia.²⁹
30. Huo ndio mwisho wao wa ujuzi. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi mwenye kuipotea njia yake, na Yeye ndiye anaye mjua zaidi mwenye kuongoka.³⁰
31. Ni vya Mwenyezi Mungu vyote viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, ili awalipe walio tenda ubaya kwa waliyo yatenda, na walio tenda mema awalipe mema.³¹
32. Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vichafu, isipo kuwa makosa khafifu. Hakika Mola wako Mlezi ni Mkunjufu wa maghfira, naye anakujueni sana tangu alipo kuumbeni kutoka kwenye ardhi, na mlipo kuwa mimba matumboni mwa mama zenu. Basi msijisifu usafi. Yeye anamjua sana mwenye kujikinga na maovu.³²
33. Je! Umemwona yule aliye geuka?³³

yoyote ya kusadikisha huo uzushi wenu mnao wadaia. Na hawa hawafuati ila ni dhana tu, na kipendacho nyoyo zao zililo potoka na kuacha maumbile yaliyo sawa. Na hakika yalikwisha wajia kutoka kwa Mola wao Mlezi yenye uwongofu, laiti wangeli ufuata huo.

24 Mwanaadamu hapati kila anacho kitamani, ya kupata uombezi wa haya masanamu au mengineyo anayo yatamani kwa nafsi yake. Kwani mambo yote, ya duniani na Akhera, ni ya Mwenyezi Mungu pekee yake.

25 Tazama tanbihi ya 24.

26 Na malaika wengi wa mbinguni, juu ya ubora wa vyeo vyao, haufai kitu uombezi wao isipo kuwa baada ya kupewa idhini huyo mwombezi na Mwenyewe Mtukufu, na kumridhia huyo mwenye kuombewa.

27 Hakika hao wasio iamani Akhera ndio bila ya shaka wanao sema kuwa Malaika ni wanawake. Wanasema: Malaika ni mabinti wa Mwenyezi Mungu!

28 Na kwa kauli hii hawana ujuzi wowote. Hawafuati kitu ila dhana zao tu zililo potoka, na dhana haifai kitu mbele ya haki.

29 Basi jitenge nao hao makafiri walio ipuza Qur'ani na ikawa hamu yao si chochote ila uhai wa duniani tu, wakiyakataa yenye maslahi nao.

30 Hayo wanayo yafuata katika itikadi zao, na vitendo vyao ndio ukomo walio yafikilia katika ilimu. Hakika Mola wako Mlezi anamjua vyema anaye shikilia upotovu, na anamjua vyema aliye elekea kupokea uwongofu.

31 Na ni vya Mwenyezi Mungu pekee vyote viliomo katika mbingu na ardhi, kwa kuviumba na kuvidabiri, ili awalipe walio potea wenye kufanya viovu vitendo vyao, na awalipe walio hidika watu wema kwa malipo yaliyo mema.

32 Wema hao ndio wale wanao jitenga na madhambi yenye adhabu kubwa kubwa, na yanayo chukiza mno. Lakini Mwenyezi Mungu husamehe dhambi ndogo ndogo. Hakika Mola wako Mlezi ni Mkuu wa kughufiria, naye anajua vyema hali zenu. Kwani Yeye ndiye aliye kuumbeni kutokana na ardhi, na mlipo kuwa mimba matumboni mwa mama zenu katika hali zenu mbali mbali za kukua na kugeuka. Basi msikae mkijisifu nafsi zenu kuwa mmesafika kwa kujigamba na kujifakhari. Na Yeye ndiye Mjuzi mkubwa kabisa wa kila mwenye kumcha na akajisafisha nafsi yake kweli kweli kwa uchungu wake.

33 Je! Umezingatia ukamwona anaye puza kuifuata Haki, na akatoa kidogo katika mali, na khalafu akakata kabisa kutoa? Je! Huyu anayo ilimu ya kujua mambo ya ghaibu, basi kwa hivyo ndio anayajua yanayo mpelekea kuiacha kuifuata Haki, na akafanya ubakhili wa mali?

34. Na akatoa kidogo, kisha akajizuia?³⁴
35. Je! Anayo huyo ilimu ya ghaibu, basi ndio anaona?³⁵
36. Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa?³⁶
37. Na vya Ibrahimu aliye timiza ahadi?³⁷
38. Ya kwamba hakika nafsi iliyo beba madhambi haibebi madhambi ya mwengine?³⁸
39. Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyo yafanya mwenyewe?³⁹
40. Na kwamba vitendo vyake vitaonekana?⁴⁰
41. Kisha ndio atalipwa malipo yake kwa ukamilifu.⁴¹
42. Na kwamba kwao Mola wako Mlezi ndio mwisho.⁴²
43. Na kwamba Yeye ndiye anaye leta kicheko na kilio.⁴³
44. Na kwamba Yeye ndiye anaye fisha na kuhuisha.⁴⁴
45. Na kwamba Yeye ndiye aliye umba jozi, dume na jike⁴⁵
46. Kutokana na mbegu ya uzazi inapo miminwa.⁴⁶
47. Na kwamba ni juu yake ufufuo mwengine.⁴⁷
48. Na kwamba ni Yeye ndiye anaye tosheleza na kukinaisha.⁴⁸
49. Na kwamba hakika Yeye ndiye Mola Mlezi wa nyota ya Shii'ra.⁴⁹
50. Na kwamba Yeye ndiye aliye waangamiza A'di wa kwanza,⁵⁰
51. Na Thamudi hakuwabakisha,⁵¹
52. Na kabla yao kaumu ya Nuhu. Na hao hakika walikuwa ni madhaalimu zaidi, na waovu zaidi;⁵²
53. Na miji iliyo pinduliwa, ni Yeye aliye ipindua.⁵³

34 Tazama tanbihi ya 33.

35 Tazama tanbihi ya 33.

36 Kwani huyo hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa na Ibrahim, aliye fika ukomo wa kutimiza aliyo agana na Mwenyezi Mungu, ya kwamba hapana mtu ataye mbebea dhambi mwengine?

37 Tazama tanbihi ya 36.

38 Tazama tanbihi ya 36.

39 Na kwamba mtu hapati ila malipo ya vitendo vyake mwenyewe.

40 Na kwamba vitendo vyake vitakuja tangazwa, na ataviona Siku ya Kiyama, iwe ni kumtukuza mtenda mema, na kumkebehi mtenda maovu.

41 Kisha kila mtu atalipwa malipo anayo stahiki.

42 Na kwamba kwa hakika ni kwa Mola wako Mlezi, wala si kwa mwengine, ndio miadi ya kurejea.

43 Na Yeye peke yake ni Mwenye uweza wa kuufanya uso uonyeshe furaha au maudhiko, na pia ni Mwenye kuziumba sababu za starehe na dhiki.

44 Na hakika ni Yeye, ndiye Mwenye kuondoa uhai, na kuuleta.

45 Na Yeye ndiye aliye umba vitu kwa jozi, yaani dume na jike, binaadamu na wanyama, kutokana na manii yanayo miminwa. (*Tazama Maelezo 53:45*)

46 Tazama tanbihi ya 45.

47 Na juu yake Yeye ndio kufufua baada ya kifo.

48 Na Yeye ndiye anaye toa kinacho tosheleza, na akaridhisha kwa kinacho kinaisha na cha kuweka akiba.

49 Na hakika Yeye ndiye Mola Mlezi wa hii nyota kubwa inayo itwa Shii'ra (Sirius, Dog Star). (*Tazama Maelezo 53:49*)

50 Na Yeye ndiye aliye wateketeza kina A'di wa mwanzo, kaumu ya Nabii Hudi. Na akawateketeza Thamudi, kaumu ya Nabii Saleh. Hakuwabakisha.

51 Tazama tanbihi ya 50.

52 Na aliwaangamiza kaumu ya Nuhu kabla ya kuwaangamiza A'di na Thamudi. Hakika hao walikuwa wamekithiri kudhulumu, na wamezidi kwa uasi kuliko A'di na Thamudi.

53 Na miji ya kaumu Lut'i iliyo pinduliwa juu chini, ni Yeye Mwenyezi Mungu ndiye aliye ipindua.

54. Vikaifunika vilivyo funika.⁵⁴
55. Basi neema gani ya Mola wako Mlezi unayo ifanyia shaka?⁵⁵
56. Hili ni Onyo katika maonyo yale yale ya zamani.⁵⁶
57. Kiyama kimekaribia!⁵⁷
58. Hapana wa kukifichua isipo kuwa Mwenyezi Mungu.⁵⁸
59. Je! Mnayastaajabia maneno haya?⁵⁹
60. Na mnacheka, wala hamlii?⁶⁰
61. Nanyi mmeghafilika?⁶¹
62. Basi msujudieni Mwenyezi Mungu, na mumuabudu.⁶²

54 Akaizunguka kwa kuiadhibu kama alivyo izunguka. Basi katika neema za Mola wako Mlezi una shaka nayo ipi?

55 Tazama tanbihi ya 54.

56 Hii Qur'ani ni onyo katika jinsi ya yale yale maonyo ya kale waliyo onywa kwayo watu walio tangulia.

57 Kiyama kimekaribia; na wala hapana wa kuujulisha wakati kitapo tokea ila mwenyewe Mwenyezi Mungu.

58 Tazama tanbihi ya 57.

59 Hivyo nyinyi mnapinga kila la kweli? Na mnaistaajabia kwa kuikaataa hii Qur'ani? Na mnacheka kwa kejeli na maskhaara, wala hamlii kama wafanyavyo wenye yakini, nanyi mmo katika pumbao na kutakabari?

60 Tazama tanbihi ya 59.

61 Tazama tanbihi ya 59.

62 Basi msujudieni Mwenyezi Mungu aliye iteremsha Qur'ani kuwa ni uwongofu kwa watu wote, na muabuduni Yeye tu peke yake Mwenye kutukuka kwa utukufu wake.

Sura 54 - Al-Qamar

Utangulizi

Imekuja Aya ya kwanza katika Sura hii kuzindua kuwa watu wasikilize kwamba Kiyama kinakaribia, na watu wanahadharishwa na tukio hilo. Kisha zimekuja Aya nyengine baada yake kuweka wazi msimamo wa makafiri kwa mintarafu ya miujiza, na kushikilia kwao kukadhibisha. Na anatakiwa Mtume s.a.w. awapuuze na awangojee mpaka siku watakapo toka makaburini kama nzige walio tapanyika.

Tena baada ya hapo Aya zikawa zinafuatana, zikieleza hali namna mbali mbali za mataifa yaliyo tangulia kwa mnasaba na Mitume wao, na adhabu iliyo washukia. Na baina ya kila kisa na kingine inazindua mawazo ya kwamba Qur'ani tukufu imefanywa nyepesi kwa mwenye kutaka kuwaidhika na kuzingatia.

Mwishoe inabainisha kwamba hao makafiri wa Makka si watu wenye nguvu zaidi au wakali zaidi kushinda mataifa yaliyo kwisha tangulia, na kwamba wao si wenye kuiepuka adhabu. Tena Sura ikakhitimisha kwa kuwahadharisha wanao kadhibisha wenye inda kuwa mwisho wao watakuja tumbukizwa Motoni kifudufudi, na wataambiwa: Onjeni mguso wa Jahannamu mliyo kuwa mkiikadhibisha. Na inawatuza wachamngu katika maskani zao za Mabustanini na mito, katika makao mazuri kwa Mfalme Mwenye uweza.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Saa imekaribia, na mwezi umepasuka!¹
2. Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: Huu uchawi tu unazidi kuendelea.²
3. Na wamekanusha na wamefuata matamano yao. Na kila jambo ni lenye kuthibiti.³
4. Na bila ya shaka zimewajia khabari zenye makaripio.⁴
5. Hikima kaamili; lakini maonyo hayafai kitu!⁵
6. Basi jiepuche nao. Siku atakapo ita mweitaji kuliendea jambo linalo chusha;⁶
7. Macho yao yatainama; watatoka makaburini kama nzige walio tawanyika,⁷
8. Wanamkimbilia mweitaji, na makafiri wanasema: Hii ni siku ngumu.⁸

1 Kiyama kimekaribia na mwezi utapasuka hapana hivi wala hivi.

2 Na makafiri wakiona Ishara, yaani muujiza mkubwa, wao hupuza wakaacha kuuamini. Bali husema: Huu ni uchawi wa daima unaendelea!

3 Na wamekanusha Mitume na wakafuata yaliyo zainishwa na matamano yao. Na kila jambo huishia mwisho wake linapo tulia na kuthibiti.

4 Na ninaapa kuwa zimewajia makafiri khabari za mataifa yaliyo tangulia zenye ukweli wa uumbaji ambazo zina mikemeo ya kutosha.

5 Haya yaliyo wajia ni hikima kubwa na lengo la kufikia mbali. Lakini maonyo yataleta faida gani kwa wanao zipinga hikima hizo?

6 Ewe Muhammad! Waachilie mbali hawa makafiri, nawe ngojea siku atapoita mweitaji wa Mwenyezi Mungu kuitia jambo ambalo nafsi inalichukia mno!

7 Macho yao yatainama chini kwa wingi wa kitisho, wakitoka makaburini kama kwamba ni nzige walio tawanyika, kwa wingi wao na mbio zao.

8 Wakimkimbilia huyo mweitaji, wakimtazama kwa unyonge na unyenekevu, macho yao yanamwanguka

9. Kabla yao kaumu ya Nuhu walikanusha; wakamkanusha mja wetu, na wakasema ni mwendawazimu, na akakaripiwa.⁹
10. Basi akamwomba Mola wake Mlezi akasema: Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru!¹⁰
11. Basi tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayo miminika.¹¹
12. Na tukazipasua ardhi kwa chemchem, yakakutana maji kwa jambo lilio kadiriwa.¹²
13. Na tukamchukua kwenye safina ya mbao na kamba.¹³
14. Ikawa inakwenda kwa nadhari yetu, kuwa ni malipo kwa alivyo kuwa amekanushwa.¹⁴
15. Na bila ya shaka tuliiacha iwe ni Ishara. Lakini je, yupo anaye kumbuka?¹⁵
16. Basi ilikuwaje adhabu yangu, na maonyo yangu.¹⁶
17. Na bila ya shaka Sisi tumeifanya Qur'ani iwe nyepesi kufahamika. Lakini yupo anaye kumbuka?¹⁷
18. Kina A'di walikanusha. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo yangu?¹⁸
19. Hakika Sisi tuliwapelekea upepo wa kimbunga katika siku korofi mfululizo,¹⁹
20. Ukiwang'oa watu kama vigogo vya mitende vilio ng'olewa.²⁰
21. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo yangu?²¹
22. Na bila ya shaka Sisi tumeifanya Qur'ani nyepesi kufahamika; lakini yupo anaye kumbuka?²²
23. Thamudi waliwakanusha Waonyaji.²³
24. Wakasema: Ati tumfuate binaadamu mmoja katika sisi? Basi hivyo sisi tutakuwa

yeye tu. Makafiri watasema Siku ya Kiyama: Hii leo ni siku nzito, siku ya shida!

9 Kabla ya makafiri wa Makka walikwisha kanusha kaumu ya Nuhu. Walimkadhibisha Nuhu, mja wetu na Mtume wetu, wakamsingizia kuwa ana wazimu. Wakaingiza baina yake na kufikisha kwake Ujumbe kila namna ya maudhi na vitisho.

10 Nuhu akamwomba Mola wake Mlezi akisema: Hakika mimi nimeshindwa na hawa watu wangu, basi wapatilize hawa kwa ajili yangu!

11 Basi tukaifungua milango ya mbingu ikamimina maji yasiyo katika; na tukaipasua ardhi kwa chemchem zikitibuka maji. Yakakutana maji ya mbinguni na maji ya ardhi kuwahiliki, kama alivyo kadiria Mwenyezi Mungu Mtukufu.

12 Tazama tanbihi ya 11.

13 Tukampakia Nuhu katika jahazi la mbao zinazo fungwa pamoja kwa kamba, kama mtepe. Likawa linakwenda baharini chini ya hifadhi yetu, kuwa ni malipo kwa Nuhu ambaye watu wake waliendelea kuukanya wito wake.

14 Tazama tanbihi ya 13.

15 Na tumeliacha hilo tukio na kuzamishwa makafiri na kuokolewa Waumini liwe ni mawaidha, lakini yupo mwenye kuwaidhika?

16 Jee, vipi ilikuwa adhabu yangu na onyo langu kwa wakhalifu.

17 Ninaapa, tumeifanya Qur'ani iwe sahali kukumbukwa na kutoa mawaidha. Lakini je, yupo na kuwaidhika?

18 Kina A'di walimkadhibisha Mtume wao Hudi. Je, hali gani adhabu yangu na onyo langu lilikuwa kwa wenda kinyume!

19 Sisi kwa yakini tuliwapatiliza kwa upepo ubaridi unao vuma, katika siku ya ukorofi wa daima, ukiwang'oa watu na kuwatupa nao wamekufa, kama vinavyo ng'olewa vigogo vya mitende na mizizi yake.

20 Tazama tanbihi ya 19.

21 Hali gani adhabu yangu na onyo langu lilikuwa kwa walio kwenda kinyume!

22 Na bila ya shaka Sisi tumeifanya sahali Qur'ani kwa ajili ya mawaidha na mazingatio, basi je, yupo wa kuwaidhika?

23 Thamudi walikadhibisha maonyo ya Nabii wao, Saleh.

katika upotofu na kichaa!²⁴

25. Ni yeye tu aliye teremshiwa huo ukumbusho kati yetu sote? Bali huyu ni mwongo mwenye kiburi!²⁵

26. Kesho watajua ni nani huyo mwongo mwenye kiburi.²⁶

27. Hakika Sisi tutawapelekea ngamia jike ili kuwajaribu, basi watazame tu na ustahamili.²⁷

28. Na waambie kwamba maji yatagawanywa baina yao; kila sehemu ya maji itahudhuriwa na aliye khusika.²⁸

29. Basi wakamwita mtu wao akaja akamchinja.²⁹

30. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo yangu!³⁰

31. Hakika Sisi tuliwapelekea ukelele mmoja tu, wakawa kama mabuwa ya kujengea uwa.³¹

32. Na bila ya shaka Sisi tumeifanya Qur'ani iwe nyepesi kwa kukumbuka, lakini yupo akumbukaye?³²

33. Kaumu Lut'i nao waliwakadhibisha Waonyaji.³³

34. Hakika Sisi tukawapelekea kimbunga cha vijjiwe, isipo kuwa wafuasi wa Lut'i. Hao tuliwaokoa karibu na alfajiri.³⁴

35. Kwa neema inayo toka kwetu. Hivyo ndivyo tumlipavyo anaye shukuru.³⁵

36. Na hakika yeye aliwaonya adhabu yetu; lakini wao waliyatilia shaka hayo maonyo.³⁶

37. Na walimtaka awape wageni wake. Tukayapofua macho yao, na tukawaambia: Onjeni basi adhabu na maonyo yangu!³⁷

38. Na ili wafikia wakati wa asubuhi adhabu yangu ya kuendelea.³⁸

24 Wakasema: Hivyo aje mtu tu katika sisi, watu wa kawaida, asiye na watu, nasi tumfuate? Tukimfuata huyo basi bila ya shaka sisi tutakuwa mbali mno na haki, na tutakuwa tuna wazimu basi.

25 Uteremshiwe wahyi kwake yeye katika sisi na hali wapo wanao stahiki zaidi? Bali huyo kazidi katika uwongo, mwenye kukanya neema.

26 Karibu watakuja jua siku itapo wateremkia adhabu ni nani mwongo anaye ikanya neema. Wao au Saleh, Mtume wao?

27 Hakika Sisi tunampelekea Mtume wetu Saleh ngamia mke, awe ni mtihani wao. Basi wangojee, na uwatazame watafanya nini. Na subiri, uvumilie maudhi yao mpaka itapo kuja amri ya Mwenyezi Mungu.

28 Na waambie kwamba maji yatagawanywa baina yao na ngamia. Kila mmoja wao atakuwa na zamu yake aje kunywa katika siku yake.

29 Wakamwita mtu wao mmoja akapania kumchinja yule ngamia, akamchinja. Basi vipi ilikuwa adhabu yangu na onyo langu kwa hao wakhalifu walio kwenda kinyume na amri.

30 Tazama tanbihi ya 29.

31 Sisi tuliwapatiliza kwa ukelele mmoja tu, wakawa kama miti mikavu anayo ikusanya yeyote atakaye kujengea boma la uwa wake.

32 Na bila ya shaka Sisi tumeisahilisha Qur'ani iwe nyepesi kwa ajili ya mawaidha na kuzingatia. Lakini je, yupo wa kuwaidhika?

33 Kaumu Lut'i nao walikadhibisha maonyo ya Mtume wao.

34 Hakika Sisi tuliwapelekea upepo mkali wa kuwatupia changarawe. Isipo kuwa watu wa Lut'i walio amini. Hao tuliwaokoa na adhabu hii mwisho wa usiku, kwa kuwapa neema iliyo toka kwetu. Neema kama hizo kubwa kubwa ndivyo tunavyo walipa wenye kuishukuru neema yetu kwa imani yao na ut'iifu.

35 Tazama tanbihi ya 34.

36 Na hakika Lut'i aliwahadharisha watu wake vipi mshiko wetu ulivyo mkali, wakatilia shaka maonyo yake kwa kuwa wanamwona mwongo.

37 Wakamtaka awape wageni wake wawatende fiili yao, tukayafuta macho yao kuwa ni malipo kwa hilo walilo litaka. Basi waambie kwa kuwakejeli: Igugumieni adhabu yangu, na maonyo yangu!

38 Na asubuhi mapema ikawashitua adhabu ya kuthibiti milele. Wakaambiwa: Igugumieni adhabu yangu

39. Basi onjeni adhabu na maonyo yangu!³⁹
40. Na hakika tumeisahilisha Qur'ani kuikumbuka. Lakini yupo anaye kumbuka?⁴⁰
41. Na Waonyaji waliwafikia watu wa Firauni.⁴¹
42. Walizikadhibisha Ishara zetu zote, nasi tukawashika kama anavyo shika Mwenye nguvu Mwenye uweza.⁴²
43. Je! Makafiri wenu ni bora kuliko hao, au yameandikwa vitabuni kuwa nyinyi hamtiwi makosani?⁴³
44. Au ndio wanasema: Sisi ni wengi tutashinda tu.⁴⁴
45. Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma.⁴⁵
46. Bali Saa ya Kiyama ndio miadi yao, na Saa hiyo ni nzito zaidi na chungu zaidi.⁴⁶
47. Hakika wakosefu wamo katika upotofu na wazimu.⁴⁷
48. Siku watakapo kokotwa Motoni kifudufudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu!⁴⁸
49. Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo.⁴⁹
50. Na amri yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.⁵⁰
51. Na bila ya shaka tumekwisha waangamiza wenzenu. Lakini yupo anaye kumbuka?⁵¹
52. Na kila jambo walilo lifanya limo vitabuni.⁵²
53. Na kila kidogo na kikubwa kimeandikwa.⁵³
54. Hakika wachamngu watakuwa katika Mabustani na mito.⁵⁴
55. Katika makalio ya haki kwa Mfalme Mwenye uweza.⁵⁵

na maonyo yangu!

39 Tazama tanbihi ya 38.

40 Na hakika tumeifanya Qur'ani ni sahali kwa ajili ya mawaidha na mazingatio. Je! Yupo anaye waidhika?

41 Na watu wa Firauni yaliwajia maonyo ya mfululizo.

42 Walikadhibisha Ishara zetu na miujiza yetu waliyo kuja nayo Mitume wetu. Tukawaangamiza kwa maangamizo ya nguvu yasiyo shindika, ya uwezo mkubwa.

43 Ati nyinyi, makafiri, mna nguvu zaidi kuliko hao wa kaumu zilizo tangulia ambao wameangamizwa? Au nyinyi mmetolewa makosani kwa ilivyo teremka katika Vitabu vya mbinguni?

44 Bali ati wanasema hawa makafiri: Sisi ni kikundi kilicho unganwa chenye nguvu juu ya maadui wake, hakishindwi.

45 Kikundi hicho kitashindwa, na watakimbia mbio wakifurushwa.

46 Bali Kiyama ndio miadi ya adhabu yao. Na Kiyama ni kizito zaidi, na kichungu zaidi.

47 Hakika wakosefu kutokana na hawa na hao watakuwa katika hilaki na Jahannamu inayo waka moto.

48 Siku watapo bururwa kifudufudi katika Moto wakiambiwa: Hilikini kwa machungu ya Jahannamu na joto lake.

49 Hakika Sisi tumeumba kila kitu. Tumeviumba kwa kukadiria inavyo hitajia hikima.

50 Na haikuwa amri yetu tukitaka kitu ila neno moja tu, nalo ni kusema: "Kuwa", nacho huwa, papo hapo kama kupepesa kwa jicho.

51 Na bila ya shaka Sisi tumekwisha waangamiza wengine walio fanana nanyi katika ukafiri. Je! Yupo aliye waidhika?

52 Na kila kitu walicho kifanya duniani kimeandikwa katika madaftari, kimeambatishwa nao.

53 Na kila dogo na kubwa katika vitendo limeandikwa. Hakipotei kitu.

54 Hakika wachamngu watakuwa katika Mabustani yenye shani kuu, na mito ya namna mbali mbali.

55 Katika baraza ya Haki, hakuna porojo huko wala madhambi, kwa Mwenyewe Mfalme Mtukufu wa uweza.

Sura 55 - Arrah'man

Utangulizi

Sura hii imeingia kuzihisabu fadhila na neema za Mwenyezi Mungu, kwa kuanzia baada ya kumtaja *Arrah'man*, Mwingi wa Rehema, kwa kutaja neema yake tukufu kabisa, nayo ni Kufunza Qur'ani Tukufu. Tena Aya zikaendelea kuzieleza hizo neema kwa namna ya kuweka wazi utukufu wa Mwenye kuziumba, aliye tukuka shani yake; na inadhihirisha uweza wake na ufalme wake juu ya wanaadamu na majini katika mbingu na ardhi.

Na inaeleza adhabu za wakosefu na wanao kadhibisha katika Jahannamu, na ikafafanua neema za wachamngu Peponi.

Na Sura ikakhitimisha kwa kumtakasa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kumsifu.

Na Sura imeikariri Aya isemayo “Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?” mara thalathini na moja, katika mpango wa ki- Qur'ani kukariri kunako pendeza kama inavyo wafikiana na haja. Kila moja katika hizo Aya inawagonga hao wakanushaji kwa kuzikadhibisha kwao neema za Mwenyezi Mungu katika Aya iliyo kabla yake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. *Arrah'man*, Mwingi wa Rehema¹
2. Amefundisha Qur'ani.²
3. Amemuumba mwanaadamu,³
4. Akamfundisha kubaini.⁴
5. Jua na mwezi huenda kwa hisabu.⁵
6. Na mimea yenye kutambaa, na miti, inanyenyekea.⁶
7. Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani,⁷
8. Ili msidhulumu katika mizani.⁸
9. Na wekeni mizani kwa haki, wala msipunje katika mizani.⁹
10. Na ardhi ameiweka kwa ajili ya viumbe.¹⁰

1 *Arrah'man*, Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema amefundisha mwanaadamu Qur'ani na akaifanya iwe nyepesi kwake kuisoma na kuifahamu.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Yeye amemuumba mwanaadamu, na akamfunza kubainisha, kudhihirisha yaliyo ndani ya nafsi yake, kinyume na makhaluku wengine.

4 Tazama tanbihi ya 3.

5 Na jua na mwezi zinakwenda katika njia zake za mbinguni kwa mujibu wa hisabu na vipimo visio kwenda pogo. (*Tazama Maelezo 55:5*)

6 Na mimea isiyo na vigogo, na miti inayo simama juu ya vigogo vyake, yote hiyo inamt'ii na kumnyenyekea Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kila alitakalo kwao.

7 Na mbingu ameziumba kwa kuziweka juu, na akaweka uadilifu ili mipaka isikiukwe.

8 Tazama tanbihi ya 7.

9 Na wekeni mizani kwa uadilifu katika kila muamala wenu, wala msipunguze mizani.

10 Na ardhi ameiunja na amewatandikia viumbe wanafiike kwayo.

11. Humo yamo matunda na mitende yenye mafumba.¹¹
12. Na nafaka zenye makapi, na rehani.¹²
13. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?¹³
14. Amemuumba mtu kwa udongo wa kinamo.¹⁴
15. Na akawaumba majini kwa ulimi wa moto.¹⁵
16. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?¹⁶
17. Mola Mlezi wa mashariki mbili na wa magharibi mbili.¹⁷
18. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?¹⁸
19. Anaziendesha bahari mbili zikutane;¹⁹
20. Baina yao kipo kizuizi, zisiingiliane.²⁰
21. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?²¹
22. Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani.²²
23. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?²³
24. Na ni vyake Yeye hivi viendavyo baharini vilivyo undwa kama vilima.²⁴
25. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?²⁵
26. Kila kilioko juu yake kitatoweka.²⁶
27. Na atabakia Mwenyewe Mola wako Mlezi Mwenye utukufu na ukarimu.²⁷
28. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?²⁸
29. Vinamwomba Yeye vilivyomo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye yumo katika mambo.²⁹

11 Katika ardhi yapo matunda ya namna nyingi, na imo mitende ambayo ina mafumba ambayo ndani yake ndio imo thamra ya hizo tende.

12 Na katika ardhi zipo nafaka zenye makapi. Hiyo ni riziki yenu na wanyama wenu. Na humo pia ipo mimea yenye harufu nzuri nzuri.

13 Neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi ambayo nyinyi, makundi mawili, watu na majini, mnaikataa?

14 Ameumba jinsi ya kiutu kwa udongo mkavu usio chomwa kama wa vyungu. Na ameumba jinsi ya kijini kutokana na ndimi za moto.

15 Tazama tanbihi ya 14.

16 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi ambayo mnaikataa?

17 Mlezi wa matokeo mawili ya jua, na Mola Mlezi wa machwea jua mawili. (*Tazama Maelezo 55:17*)

18 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

19 Mwenyezi Mungu anazipeleka bahari mbili, ya maji matamu na maji ya chumvi, yanakaribiana bali yanagusana khasa juu yao. Lakini baina yao kipo kizuizi kwa kudra ya Mwenyezi Mungu, kinacho zuia yasichanganyikane.

20 Tazama tanbihi ya 19.

21 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

22 Humo hutoka lulu na marijani mnazo zifanya kuwa ni pambo la kulivaa. (*Tazama maoni ya wataalamu juu ya Aya 12, Sura 35, Faat'ir.*)

23 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

24 Na yake Yeye majahazi yaliyo undwa kwa mikono yenu, yanayo kwenda baharini, makubwa yamenyanyuka juu kama vilima.

25 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

26 Kila kilioko juu ya ardhi kitaondoka, na atakabakia Mwenyezi Mungu tu, Mwenye utukufu na kuneemesha.

27 Tazama tanbihi ya 26.

28 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

29 Wote waliomo mbinguni na waliomo katika ardhi wanamwomba haja zao Mwenyezi Mungu. Kila

30. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?³⁰
31. Tutakuhisabuni enyi makundi mawili.³¹
32. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?³²
33. Enyi makundi ya majini na watu! Mkiweza kupenya kwenye mbingu na ardhi, basi penyeni! Hamtapenya ila kwa kupewa madaraka.³³
34. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?³⁴
35. Mtapelekewa muwako wa moto na shaba; wala hamtashinda.³⁵
36. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?³⁶
37. Itakapo pasuka mbingu ikawa nyekundu kama mafuta.³⁷
38. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?³⁸
39. Siku hiyo hataulizwa dhambi zake mtu wala jini.³⁹
40. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁴⁰
41. Watajuulikana wakosefu kwa alama zao, basi watashikwa kwa nywele zao za utosini na kwa miguu.⁴¹
42. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁴²
43. Hii ndiyo Jahannamu ambayo wakosefu wakiikanusha.⁴³
44. Watakuwa wakizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayo chemka.⁴⁴
45. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁴⁵
46. Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi atapata Bustani mbili.⁴⁶
47. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁴⁷
48. Bustani zenye matawi yaliyo tanda.⁴⁸

wakati Yeye yumo katika jambo, hutukuza na huangusha, hutoa na hunyima

30 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

31 Tutakushughulikieni kwa kukusudia kukuhisabieni, enyi majini na watu Siku ya Kiyama.

32 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

33 Enyi makundi ya majini na watu! Ikiwa mnaweza kutoka pembezoni mwa mbingu na ardhi kwa kukimbia, basi haya tokeni! Lakini hamwezi kutoka ila kwa nguvu na kahari; na hayo hamna uwezo nayo!
(Tazama Maelezo 55:33)

34 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

35 Mtamiminiwa ndimi za moto na shaba iliyo yayushwa, basi hamtaweza kujilinda na adhabu hiyo.
(Tazama Maelezo 55:35)

36 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

37 Siku itapo pasuka mbingu ikawa nyekundu iliyo tibuka kama mafuta yanayo unguu.

38 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

39 Basi siku itapo pasuka mbingu, siku hiyo haulizwi mtu wala jini dhambi zake.

40 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

41 Wakosefu miongoni mwa watu na majini watajuulikana kwa alama za kuwatambulisha. Basi watakatwa washikwe kwa nywele za utosi na kwa miguu watumbukizwe katika Jahannamu!

42 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

43 Wataambiwa kwa kuwashitua: Hii ndiyo Jahannamu waliyo kuwa wakiikadhibisha wakosefu miongoni mwenu. Watakuwa wakizunguka baina ya moto na maji ya ukomo wa kuchemka.

44 Tazama tanbihi ya 43.

45 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

46 Na mwenye kukhofu uweza wa Mola wake Mlezi atakuwa nazo Bustani mbili.

47 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

48 Bustani hizo zina matawi ya kufurahisha mazuri.

49. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁴⁹
50. Ndani yake zimo chemchem mbili zinazo pita.⁵⁰
51. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁵¹
52. Humo katika kila matunda zimo namna mbili.⁵²
53. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁵³
54. Wawe wameegemea matandiko yenye bit'ana ya hariri nzito; na matunda ya Bustani hizo yapo karibu.⁵⁴
55. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁵⁵
56. Humo watakuwamo wanawake watulizao macho yao; hajawagusa mtu kabla yao wala jini.⁵⁶
57. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁵⁷
58. Kama kwamba wao ni yakuti na marijani.⁵⁸
59. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁵⁹
60. Ati yaweza kuwa malipo ya ihsani ila ihsani?⁶⁰
61. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁶¹
62. Na zaidi ya hizo zipo Bustani nyengine mbili.⁶²
63. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁶³
64. Za kijani kibivu.⁶⁴
65. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁶⁵
66. Na chemchem mbili zinazo furika.⁶⁶
67. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁶⁷
68. Imo humo miti ya matunda, na mitende na mikomamanga.⁶⁸
69. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁶⁹
70. Humo wamo wanawake wema wazuri.⁷⁰

49 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

50 Katika Bustani hizo mtakuwa na chemchem zinazo pita maji kama wapendavyo.

51 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

52 Humo mtakuwa namna mbili ya kila matunda.

53 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

54 Wametegemea na kutua juu ya matandiko ambayo bit'ana yao ni ya at'ilasi, hariri nzito; na matunda ya hizo Bustani mbili yatakuwa karibu kwa mwenye kuyachuma.

55 . Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

56 Katika hizo Bustani watakuwamo wake wenye kuhifadhi macho yao hawawaangalii ila waume zao tu, walio bikra hawajakaribiwa kabla yao na mtu wala jini.

57 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

58 Wanawake hao kwa uzuri wao na usafi wao wa rangi ni kama yakuti na marijani.

59 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

60 Malipo ya vitendo vyema hayawezi kuwa ila kwa thawabu njema.

61 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

62 Na mbali ya Bustani hizo zilizo kwisha tajwa, zipo mbili nyenginezo.

63 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

64 Za kijani, iliyo koza mno rangi yake hata ikawa inaingia katika weusi.

65 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

66 Ndani humo zimo chemchem mbili zinazo furika maji yasiyo katika.

67 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

68 Humo itakuwamo miti ya matunda mbali mbali, na mitende, na mikomamanga. (mikudhumani).

(Tazama Maelezo 55:68)

69 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

70 Humo watakuwamo wake wenye tabia njema, wenye nyuso za kupendeza.

71. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁷¹
72. Wanawake wazuri wanao tawishwa katika makhema.⁷²
73. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁷³
74. Hajawagusa mtu wala jini kabla yao.⁷⁴
75. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁷⁵
76. Wameegemea juu ya matakia ya kijani na mazulia mazuri.⁷⁶
77. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikanusha?⁷⁷
78. Limetukuka jina la Mola wako Mlezi Mwenye utukufu na ukarimu.⁷⁸

71 Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

72 Wazuri wa macho, wenye kutawishwa ndani ya makhema yao.

73 . Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

74 Hawajakaribiwa na mtu wala jini kabla ya waume wao.

75 . Basi neema ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

76 Wameegemea juu ya viti vya enzi vyenye makava ya kijani na mazulia mazuri mazuri yaliyo fanywa kwa ufundi wa ajabu.

77 Basi neema ipi katika neemza za Mola wenu Mlezi mnayo ikataa?

78 Limetakasika jina la Mola wako Mlezi Mwenye utukufu na wingi wa neema.

Sura 56 - Al-Waaqia'h

Utangulizi

Sura hii imeanzia kwa kusimulia Tukio la Kiyama, na matokeo yatayo ambatana na Tukio hilo. Kisha ikasimulia kuwa viumbe Siku hiyo watakuwa namna tatu. Ikafuatia hayo kwa kufafanua kwa kutosha walio andaliwa kila fungu katika hao, ikiwa ni neema zinazo wafikiana na cheo chao, au ni adhabu inayo nasibiana na ukafiri wao na uasi wao.

Kisha Aya zikaweka wazi baada ya hayo yanayo onekana katika neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na athari za uweza wake katika viumbe, na makulima, na maji, na moto; na yanayo hitajika kutokana na athari hizi kumsabihi Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumtakasa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Litakapo tukia hilo Tukio¹
2. Hapana cha kukanusha kutukia kwake.²
3. Literemshalo linyanyualo,³
4. Itakapo tikiswa ardhi kwa mtikiso,⁴
5. Na milima itapo sagwasagwa,⁵
6. Iwe mavumbi yanayo peperushwa,⁶
7. Na nyinyi mtakuwa namna tatu:-⁷
8. Basi watakuwepo wa kuliani; je, ni wepi wa kuliani?⁸
9. Na wa kushotoni; je, ni wepi wa kushotoni?⁹
10. Na wa mbele watakuwa mbele.¹⁰
11. Hao ndio watakao karibishwa¹¹
12. Katika Bustani zenye neema.¹²

1 Kitakapo tukia Kiyama haitatokea nafsi yoyote ya kukadhibisha kutukia kwake. Kiyama hicho kitawateremsha chini walio waovu, na kitawanyanyua juu walio wema.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Ardhi itakapo tikiswa, na ikatetemeshwa kwa nguvu, na milima ikavurugwa teketeke, ikawa vumbi la kupeperushwa. (*Tazama* Maelezo 56:4)

5 Tazama tanbihi ya 4.

6 Tazama tanbihi ya 4.

7 Na mkawa nyote siku hiyo namna tatu kwa mujibu wa vitendo vyenu;

8 Basi watu wa mkono wa kulia, watu wa cheo kilio bora, utukufu ulioje huo wa hali yao! Na watu wa kushotoni, hao ni watu wa cheo duni, uovu ulioje wa hali yao!

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Na walio tangulia mbele katika mambo ya kheri duniani ndio watakuwa mbele katika vyeo vya Akhera. Hao ndio walio karibishwa mbele kwa Mwenyezi Mungu. Mola wao Mlezi atawatia katika Bustani zenye neema.

11 Tazama tanbihi ya 10.

12 Tazama tanbihi ya 10.

13. Fungu kubwa katika wa mwanzo,¹³
14. Na wachache katika wa mwisho.¹⁴
15. Watakuwa juu ya viti vya fakhari vilivyo tonewa.¹⁵
16. Wakiviegemea wakielekeana.¹⁶
17. Wakitumikiwa na wavulana wa ujana wa milele,¹⁷
18. Kwa vikombe na mabirika na bilauri za vinywaji kutoka chemchem safi.¹⁸
19. Hawataumwa kichwa kwa vinywaji hivyo wala hawatoleweshwa.¹⁹
20. Na matunda wayapendayo,²⁰
21. Na nyama za ndege kama wanavyo tamani.²¹
22. Na Mahurulaini,²²
23. Walio kama mfano wa lulu zililo hifadhiwa.²³
24. Ni malipo kwa waliyo kuwa wakiyatenda.²⁴
25. Humo hawatasikia porojo wala maneno ya dhambi,²⁵
26. Isipo kuwa maneno ya Salama, Salama.²⁶
27. Na wale wa mkono wa kulia, ni yepi yatakuwa ya wa kuliani?²⁷
28. Katika mikunazi isiyo na miba,²⁸
29. Na migomba iliyo pangiliwa,²⁹
30. Na kivuli kilicho tanda,³⁰
31. Na maji yanayo miminika,³¹

13 Hawa walio karibishwa mbele ni kundi la wengi katika mataifa yaliyo tangulia na Manabii wao, na wachache katika umma wa Muhammad ukiwalinganisha na hao.

14 Tazama tanbihi ya 13.

15 Juu ya viti au vitanda vilivyo nakishiwa kwa nakshi za vito vya thamani, wakiviegemea kwa raha na utulivu huku wakielekezana nyuso kwa ziada ya mahaba.

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Wakiwazungukia kwa kuwakhudumia vijana watakao baki milele hivyo hivyo, nao wamechukua vikombe na mabirika yaliyo jaa vinywaji vya Peponi, na bilauri zenye mvinyo kutoka chemchem zinazo miminika,

18 Tazama tanbihi ya 17.

19 Vinywaji hivyo haviwaletei kuumwa kichwa wala kutokwa akili kwa ulevi.

20 Na matunda ya kila namna wanayo yapenda na wanayo yaona; na nyama za ndege kama zinavyo tamani nafsi zao.

21 Tazama tanbihi ya 20.

22 Na wanawake wenye macho ya vikombe, kama mfano wa lulu zililo hifadhiwa katika chaza, kwa usafi wao na urembo wao. Watapewa haya kuwa ni malipo kwa mambo mema waliyo kuwa wakiyatenda duniani.

23 Tazama tanbihi ya 22.

24 Tazama tanbihi ya 22.

25 Huko Peponi hawatasikia maneno yasiyo kuwa na maana, wala masimulizi ya kumtia dhambini mwenye kuyasikia. Ila watalo sikia ni kauli ya wao kwa wao: Tunakusalimuni kwa Salama.

26 Tazama tanbihi ya 25.

27 Na watu wa mkono wa kulia, hapana ajuaye nini malipo ya watu wa kuliani.

28 Katika miti ya mikunazi iliyo katwa miba yake, na migomba iliyo pangika na ndizi zake zimepandana juu ya mikungu, na kivuli kilicho enea wala hakiondoki, na maji yanayo miminika karibu yao popote wayatakapo, na matunda ya namna nyingi na kabila nyingi yasiyo tindikia wakati wowote, wala hazuiwiliwi ayatakayo, na matandiko yaliyo nyanyuliwa ya starehe.

29 Tazama tanbihi ya 28.

30 Tazama tanbihi ya 28.

31 Tazama tanbihi ya 28.

32. Na matunda mengi,³²
33. Hayatindikii wala hayakatazwi,³³
34. Na matandiko yaliyo nyanyuliwa.³⁴
35. Hakika Sisi tutawaumba (Mahurulaini) upya,³⁵
36. Na tutawafanya vijana,³⁶
37. Wanapendana na waume zao, hirimu moja.³⁷
38. Kwa ajili ya watu wa kuliani.³⁸
39. Fungu kubwa katika wa mwanzo,³⁹
40. Na fungu kubwa katika wa mwisho.⁴⁰
41. Na watu wa kushotoni; je ni yepi ya wa kushotoni?⁴¹
42. Katika upepo wa moto, na maji yanayo chemka,⁴²
43. Na kivuli cha moshi mweusi,⁴³
44. Si cha kuburudisha wala kustarehesha.⁴⁴
45. Hakika hao walikuwa kabla ya haya wakiishi maisha ya anasa.⁴⁵
46. Na walikuwa wakishikilia kufanya madhambi makubwa,⁴⁶
47. Na walikuwa wakisema: Tutakapo kufa na tukawa udongo na mafupa, ati ndio tutafufuliwa?⁴⁷
48. Au baba zetu wa zamani?⁴⁸
49. Sema: Hakika wa zamani na wa mwisho⁴⁹
50. Bila ya shaka watakusanywa kwa wakati wa siku maalumu.⁵⁰

32 Tazama tanbihi ya 28.

33 Tazama tanbihi ya 28.

34 Tazama tanbihi ya 28.

35 Hakika Sisi tulianza kuwaumba Mahurulaini mwanzo, na tukawafanya kuwa ni vijana, wenye kupendwa na waume zao, wenye umri ulio karibiana, wa tayari kwa neema ya watu wa kuliani.

36 Tazama tanbihi ya 35.

37 Tazama tanbihi ya 35.

38 Tazama tanbihi ya 35.

39 Watu wa kulia ni wengi katika mataifu yaliyo kwisha tangulia, na kikundi kikubwa katika umma wa Muhammad.

40 Tazama tanbihi ya 39.

41 Na watu wa kushoto, hapana anaye jua nini adhabu ya watu wa kushoto.

42 Watakuwa kwenye upepo umoto utakao wazunguka, unao penya katika tundu za mwili, na maji yaliyo chemshwa motoni wayanywe na wamiminiwe vichwani, na katika kivuli cha kiza cheusi cha moshi umoto, hapana ubaridi wa kupunguza joto la hewa, wala huruma ya kuwaletea nafuu wanapo vuta pumzi.

43 Tazama tanbihi ya 42.

44 Tazama tanbihi ya 42.

45 Hakika hao kabla ya haya walikuwa wamepita kiasi katika kustareheha neema za duniani, wamepumbaa hawataki kumt'ii Mwenyezi Mungu Mtukufu.

46 Na walikuwa wameshikilia daima kufanya dhambi kubwa kabisa, kwani waliapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba kabisa Mwenyezi Mungu hatamfufua aliye kufa.

47 Na walikuwa wakisema kwa kukanusha kurejea tena: Ati tutafufuliwa baada ya kwisha kufa, na baadhi ya miili yetu ikisha kuwa udongo na mengine mifupa iliyo chakaa? Ati sisi tutarudishwa tuwe hai mara ya pili?

48 Ati tutafufuliwa sisi na baba zetu wa zamani walio kwisha kuwa udongo ulio tapanyika na umepotea katika ardhi?

49 Waambie kwa kuwajibu kukanusha kwao: Hakika wa zamani na wa mwisho, ambao nyinyi ni katika jumla ya hao, nyote mtakusanywa katika wakati wa siku maalumu, na wala hamtoipita.

50 Tazama tanbihi ya 49.

51. Kisha nyinyi, mlio potea, mnao kanusha,⁵¹
52. Kwa yakini mtakula mti wa Zaqqumu.⁵²
53. Na kwa mti huo mtajaza matumbo.⁵³
54. Na juu yake mtakunywa maji yanayo chemka.⁵⁴
55. Tena mtakunywa kama wanavyo kunywa ngamia wenye kiu.⁵⁵
56. Hiyo ndiyo karamu yao Siku ya Malipo.⁵⁶
57. Sisi tumekuumbeni; basi hamsadiki?⁵⁷
58. Je! Mnaiona mbegu ya uzazi mnayo idondokeza?⁵⁸
59. Je! Mnaiumba nyinyi, au ni Sisi ndio Waumbaji?⁵⁹
60. Sisi tumekuwekeeni mauti; na wala Sisi hatushindwi⁶⁰
61. Kuwaleta wengine badala yenu na kukuumbeni nyinyi kwa umbo msilo lijua.⁶¹
62. Na bila ya shaka mlikwisha jua umbo la kwanza, basi kwa nini hamkumbuki?⁶²
63. Je! Mnaona makulima mnayo yapanda?⁶³
64. Je! Ni nyinyi mnayo yaotesha au ni Sisi ndio wenye kuotesha?⁶⁴
65. Tungeli taka tungeli yafanya yakawa mapepe, mkabaki mnastaajabu,⁶⁵
66. Mkisema: Hakika sisi tumegharimika,⁶⁶
67. Bali sisi tumenyimwa.⁶⁷
68. Je! Mnayaona maji mnayo yanywa?⁶⁸
69. Je! Ni nyinyi mnayo yateremsha kutoka mawinguni au ni Sisi ndio wenye

51 Kisha nyinyi, enyi mnao ipinga Njia ya Uwongofu, mnao kanusha kufufuliwa, bila ya shaka mtakula mti wa Zaqqumu katika Jahannamu, na mtajajaza matumbo yenu kwa shida ya njaa.

52 Tazama tanbihi ya 51.

53 Tazama tanbihi ya 51.

54 Mtakunywa juu ya mlichio kila maji yenye kutokota, yasiyo ondoa kiu, na mtakunywa kwa wingi na pupa kama anavyo kunywa ngamia mwenye kiu kisicho katika kiu chake kwa maj.

55 Tazama tanbihi ya 54.

56 Hayo yaliyo tajwa ya mateso mbali mbali ndio karamu yao waliyo andaliwa kwa siku ya malipo.

57 Sisi tulianza kukuumbeni mlipo kuwa si chochote, basi hebu hamkiri uweza wetu wa kukurejesheni tena baada ya kukufufueni?

58 Hamuangalii manii mnayo itia katika tumbo la uzazi? Ni nyinyi ndio mwenye uweza juu yake na kuilea mpaka ikawa mtu, au ni Sisi ndio twenye makadara hayo?

59 Tazama tanbihi ya 58.

60 Sisi tumekuhukumieni mauti, na tumeweka wakati makhsusi wa kufa kwenu. Na wala Sisi si wenye kushindwa kukubadilisheni sura zenu, na kuzileta nyengine, na tukakuumbeni katika umbo jengine na sura nyengine msiyo ijua.

61 Tazama tanbihi ya 60.

62 Bila ya shaka mmekwisha yakinika kuwa Mwenyezi Mungu alikuumbeni mara ya kwanza, basi je, hamkumbuki kwamba Mwenye kuweza hayo ni Mweza zaidi wa kufanya tena.

63 Je! Hamuangalii mbegu mnayo ipanda katika ardhi? Ni nyinyi mnao ifanya imee au ni Sisi peke yetu ndio tunaifanya imee?

64 Tazama tanbihi ya 63.

65 Tungeli taka tungeli ifanya mimea hiyo iwe mabua na mapepe yaliyo katika katika kabla haijapevuka, mkawa mkistaajabu tu kwa uovu ulio isibu, huku mkisema: Hakika sisi tumepata khasara baada ya juhudi yetu. Bali sisi hatuna bahati, tumenyimwa riziki.

66 Tazama tanbihi ya 65.

67 Tazama tanbihi ya 65.

68 Je! Hamyaoni maji matamu mnayo yanywa? Ni nyinyi mnayo yateremsha kutoka mawinguni, au ni Sisi ndio Wenye kuyateremsha kuwa ni rehema juu yenu? (*Tazama Maelezo 56:68*)

kuyateremsha?⁶⁹

70. Tungeli penda tungeli yafanya ya chumvi. Basi mbona hamshukuru?⁷⁰

71. Je! Mnauona moto mnao uwasha?⁷¹

72. Ni nyinyi mlio uumba mti wake au Sisi ndio Waumbaji?⁷²

73. Sisi tumeufanya uwe ni ukumbusho na manufaa kwa walioko nyikani.⁷³

74. Basi litakase jina la Mola wako Mlezi aliye Mkuu.⁷⁴

75. Basi naapa kwa maanguko ya nyota,⁷⁵

76. Na hakika bila ya shaka hichi ni kiapo kikubwa, laiti mngeli jua!⁷⁶

77. Hakika hii bila ya shaka ni Qur'ani Tukufu,⁷⁷

78. Katika Kitabu kilicho hifadhiwa.⁷⁸

79. Hapana akigusaye ila walio takaswa.⁷⁹

80. Ni uteremsho unao toka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁸⁰

81. Ni maneno haya ndiyo nyinyi mnayapuuza?⁸¹

82. Na badala ya kushukuru kwa riziki yenu mnafanya kuwa mnakadhibisha?⁸²

83. Yawaje basi itakapo fika roho kwenye koo,⁸³

84. Na nyinyi wakati huo mnatazama!⁸⁴

85. Na Sisi tuko karibu zaidi naye kuliko nyinyi wala nyinyi hamuoni.⁸⁵

86. Na lau kuwa nyinyi hamumo katika mamlaka yangu,⁸⁶

69 Tazama tanbihi ya 68..

70 . Lau tungeli taka tungeli yafanya hayo maji yakawa ya chumvi yasiyo nyweka. Basi mbona hamumshukuru Mwenyezi Mungu aliye yajaalia matamu yenye kunyweka?

71 Je! Hamuoni moto huo mnao uasha? Ni nyinyi ndio mlio uotesha mti wake, na mkautia ndani ya huo mti moto, au ni Sisi ndio tulio uumbia hivyo, kadhaalika?

72 Tazama tanbihi ya 71.

73 Sisi tumeufanya huu moto uwe ni ukumbusho wa Moto wa Jahannamu mtapo uona, na uwe ni manufaa kwa wasafiri wa msitu na nyika, wakinafiika kwa kupikia chakula chao na kuotea moto wakati wa baridi.

74 Basi dumisha kusabihi, kutakasa, kwa kulidhukuru jina la Mola wako Mlezi aliye Mkubwa, kwa kumtakasa na kumshukuru kwa neema hizi nzuri.

75 Basi ninaapa kweli kwa maanguko ya nyota pale zinapo tua mwisho wa usiku wakati wa Tahajudi, ibada za usiku, na kustaghafiru. Na hakika bila ya shaka hicho ni kiapo kikubwa chenye maana ya kufikia mbali, lau kuwa mnafikiri makusudio yake. (*Tazama Maelezo 56:75*)

76 Tazama tanbihi ya 75.

77 Hakika hii bila ya shaka ni Qur'ani yenye manufaa mengi, imo katika ubao ulio hifadhiwa *Al-lauhu-lmahfudh*, usio karibiwa na yeyote ila Malaika walio karibishwa kwa Mwenyezi Mungu. (Kwa watumiaji Computer wanaweza kukisia kuwa hiyo *Al-lauhu-lmahfudh* ni kama *Disk* iliyomo ndani ya Computer na haigusi mtu, na Misahafu tunayo iona, na kuisoma, ni kama yapigwayo chapa kutoka hiyo *Disk*.)

78 Tazama tanbihi ya 77.

79 Hawaigusi Qur'ani Tukufu ila walio t'ahirika na najisi na hadathi, vitengua udhu; imeteremshwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe vyote.

80 Tazama tanbihi ya 79.

81 Je! Mnapuuza? Ni Qur'ani hii tukufu ndio nyinyi mnaidharau?

82 Na badala ya kuishukuru riziki yenu ndio mna ikadhibisha?

83 Basi je! Ikifika roho ya mmoja wenu kwenye mapitio ya pumzi, na nyinyi inapo fika roho kwenye koo nanyi mnamwangalia huyo anaye kufa, na Sisi tuko karibu zaidi kwa huyo aliye kabiliwa na mauti na tunajua zaidi hali yake kuliko nyinyi, lakini nyinyi hamjui hayo wala hamhisi.

84 Tazama tanbihi ya 83.

85 Tazama tanbihi ya 83.

86 Basi je! Ikiwa nyinyi si wenye kunyenyekea kwa Ungu wetu, mrudishieni roho yake huyo aliye kabiliwa na mauti ikiwa nyinyi mwasema kweli kwamba nyinyi mnazo nguvu na hamshindwi.

87. Kwanini hamuirudishi hiyo roho, ikiwa nyinyi mnasema kweli?⁸⁷
88. Basi akiwa miongoni mwa walio karibishwa,⁸⁸
89. Basi ni raha, na manukato, na Bustani zenye neema.⁸⁹
90. Na akiwa katika watu wa upande wa kulia,⁹⁰
91. Basi ni Salamu kwako uliye miongoni mwa watu wa upande wa kulia.⁹¹
92. Na ama akiwa katika walio kadhibisha wapotovu,⁹²
93. Basi karamu yake ni maji yanayo chemka,⁹³
94. Na kutiwa Motoni.⁹⁴
95. Hakika hii ndiyo haki yenye yakini.⁹⁵
96. Basi litakase jina la Mola wako Mlezi aliye Mkubwa.⁹⁶

87 Tazama tanbihi ya 86.

88 Ama akiwa huyo aliye kabiliwa na mauti ni katika walio tangulia walio karibishwa basi mwisho wake ni raha, na rehema, na riziki njema, na Pepo yenye neema

89 Tazama tanbihi ya 88.

90 Ama akiwa katika watu wa mkono wa kulia, basi ataambiwa kwa maamkio na takrima: Unapewa salamu kutokana na watu wa kuliani.

91 Tazama tanbihi ya 90.

92 Na ama akiwa ni katika wa kushoto, wanao kanusha, walio wapotovu, basi atakirimiwa maji ya moto hadi ya kuchemka, na kubabuliwa na moto wa mwisho wa ukali.

93 Tazama tanbihi ya 92.

94 Tazama tanbihi ya 92.

95 Hakika haya yaliyo tajwa katika Sura hii tukufu bila ya shaka ni kiini cha yakini iliyo thibiti, isiyo ingiliwa na shaka.

96 Tanguliza tasbihi kwa kumdhukuru Mola wako Mlezi aliye Mkubwa, kwa kumtakasa na kumshukuru kwa neema zake.

Sura 57 - Al-H'adiid

Utangulizi

Sura hii imeanzia kwa kueleza kwamba wote walioko mbinguni na katika ardhi wamemsabihi na kumtakasa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kila kisicho kuwa laiki naye. Kisha ikafuatiliza hayo kwa kuelekeana na kusabihi huko ufalme wa mbingu na ardhi, na kuvizunguka vyote hivyo na kuviendesha. Kisha Sura ikaamrisha Imani ya Mwenyezi Mungu, na kutoa katika njia yake, na ikabainisha khitilafu za daraja za kutoa kwa mujibu wa kukhtalifiana haja ziliopo na dharura zake. Kisha ikaeleza sura ya Waumini Siku ya Kiyama, inavyo tangulia nuru yao mbele yao na pembezoni mwao; na sura ya wanafiki wanavyo waomba Waumini wawangojee ili nao wapate mwangaza kutokana na nuru yao. Na baina yao umesimamishwa ukuta wenye mlango. Ndani yake ipo rehema, na nje yake upande wa mbele yake ni adhabu.

Na Sura ikaingia baada ya hayo kuwahimiza Waumini wanyenyekee kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu, na Haki aliyo iteremsha. Na inawaonyesha vyeo vya wanao sadiki wanaume na wanawake mbele ya Mola wao Mlezi; na mwisho wa Makafiri wanao kadhibisha ni katika Jahannamu. Na inapiga mifano ya udhalili wa dunia na hizo starehe zake, na ukubwa wa Akhera na neema na adhabu zilioko huko. Na Sura inataka watu wawanie kushindania maghfira kwa Mwenyezi Mungu, na inazitua nafsi kwamba kila kinacho msibu mtu ikiwa kheri au shari kimeandikwa katika Kitabu kilichoko kwa Mwenyezi Mungu, ili nyoyo zinyenyekee kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu. Kisha ikasimulia khabari za kuwatuma Mitume na kuwafuatiliza mmoja baada ya mmoja wakipewa nguvu kwa hoja na Vitabu, na njia za nguvu na vitendo, ili watu wasimamishu uadilifu. Kisha Aya ikakhitimisha kwa kuwaita Waumini wamche Mungu, na ikawaahidi kuwa watapewa rehema maradufu na watafanyiwa hisani ya kufadhiliwa, ambayo hapana mwenye kuiweza hata kidogo ila Mwenyezi Mungu. Kwani hakika fadhila zote zimo katika mkono wa Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye fadhila kuu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Kinamsabihi kumtakasa Mwenyezi Mungu kila kiliomo ndani ya mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹
2. Yeye ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Anahuisha na anafisha. Na Yeye ni Mwenye uweza wa kila kitu.²
3. Yeye ndiye wa Mwanzo na ndiye wa Mwisho, naye ndiye wa Dhaahiri na wa Siri,

1 Mwenyezi Mungu Mtukufu anatakaswa na kila kiliomo katika mbingu na ardhi, tangu watu, na wanyama, na hata vitu visio na roho. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, anaye yaendesha mambo yote kwa mujibu wa hikima yake.

2 Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu, si wa mwenginewe. Yeye huyasarifu apendavyo yote yaliomo humo, Yeye ndiye Mwenye kuhuisha na kufisha. Na kwa kila kitu Yeye ndiye Mwenye uweza ulio timia.

naye ndiye Mjuzi wa kila kitu.³

4. Yeye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita; kisha akakaa vyema juu ya enzi. Anayajua yanayo ingia katika ardhi na yanayo toka humo, na yanayo teremka kutoka mbinguni, na yanayo panda humo. Naye yu pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona mnayo yatenda.⁴

5. Ufalme wa mbingu na ardhi ni wake. Na mambo yote yanarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.⁵

6. Anaingiza usiku katika mchana, na anaingiza mchana katika usiku. Na Yeye ni Mwenye kuyajua yaliomo vifuani.⁶

7. Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na toeni katika alivyo kufanyeni nyinyi kuwa ni waangalizi wake. Basi walio amini miongoni mwenu, na wakatoa, wana malipo makubwa.⁷

8. Na mna nini hata hamumuamini Mwenyezi Mungu na hali Mtume anakuiteni mumuamini Mola wenu Mlezi? Naye amekwisha chukua ahadi yenu, ikiwa nyinyi ni Waumini.⁸

9. Yeye ndiye anaye mteremshia mja wake Aya zinazo bainisha wazi ili akutoeni gizani muingie kwenye nuru. Na hakika Mwenyezi Mungu kwenu ni Mpole, Mwenye kurehemu.⁹

10. Na mna nini hata hamtoi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya Ushindi na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao walio toa baadae na wakapigana. Na wote hao Mwenyezi Mungu amewaahidia wema. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.¹⁰

3 Yeye alikuwapo kabla ya kila kitu, na atabaki baada ya kutoweka kila kitu. Yeye ndiye aliye dhaahiri, anaonekana, katika kila kitu. Kwani kila kitu ni Ishara yake. Na Yeye ndiye wa ndani, ambaye hawezi kueleweka kwa macho. Na Yeye ni Mwenye kutimia ujuzi wake kwa kila kitu kilicho dhaahiri na kilicho fichikana.

4 Yeye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi na viliomo kati yao kwa siku sita, kisha akakalia A'rshi (Kiti chake cha enzi) akiangalia ufalme wake. Anajua kila kinacho ghibu katika ardhi na kinacho toka humo, na kila kinacho teremka kutoka mbinguni, na kinacho panda kwendea huko. Na Yeye ni Mwenye kukujueni, anayajua vyema mambo yenu popote pale mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona myatendayo, anayajua vilivyo, wala hakifichiki kitu kwake.

5 Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu peke yake. Na kwake Yeye Mtukufu ndiye mambo ya viumbe vyake yanarejeshwa, na kwake ndiko kunako kwishia mwisho wao.

6 Yeye huziingiza saa za usiku katika mchana, na huziingiza saa za mchana katika usiku. Kwa hivyo hupatikana khitilafu katika urefu wao. Na Yeye ndiye Mjuzi wa yanayo hifadhiwa na vifua, na yanayo dhamiriwa na nyoyo.

7 Msadikini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mtoe katika *Sabilillahi*, Njia ya Mwenyezi Mungu, katika mali aliyo kujaalieni Mwenyezi Mungu nyinyi kuwa ni waangalizi katika matumizi yake. Basi hao wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake miongoni mwenu, na wakatoa katika alivyo wapa uangalizi juu yake, watapata kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya hayo malipo makubwa.

8 Na kwa nini hamumuamini Mwenyezi Mungu, na hali Mtume anakutakeni mumuamini Mola wenu Mlezi, na anakuhimizeni kwa hayo. Na Mwenyezi Mungu kesho chukua agano lenu la Imani kabla yake. Kama kweli mnaitaka Imani basi hoja zake zimekwisha thibiti.

9 Yeye ndiye anaye mteremshia Mtume wake Aya za Qur'ani zilizo wazi, ili akutoeni kwenye upotovu mwende kwenye uwongofu. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa upole kwenu, Mkunjufu wa rehema.

10 Na limekupatani nini hata hamtoi kwa ajili ya Njia ya Mwenyezi Mungu katika mali yenu, na hali Mwenyezi Mungu ndiye wa kurithi mbingu na ardhi? Yeye atarithi kila kilimo humo, wala hatabaki

11. Ni nani atakaye mkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, ili amrudishie mardufu, na apate malipo ya ukarimu.¹¹

12. Siku utakapo waona Waumini wanaume na Waumini wanawake, nuru yao iko mbele yao, na kuliani kwao: Furaha yenu leo - Bustani zipitazo mito kati yake mtakaa humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.¹²

13. Siku wanaafiki wanaume na wanaafiki wanawake watapo waambia walio amini: Tungojeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu. Waambiwe: Rejeeni nyuma yenu mkaitafute nuru! Utiwe baina yao ukuta wenye mlango - ndani yake mna rehema, na nje upande wake wa mbele kuna adhabu.¹³

14. Watawaita wawaambie: Kwani vile hatukuwa pamoja nanyi? Watawaambia: Ndiyo, lakini mlifitini wenyewe, na mkasitasita, na mkatia shaka, na matamanio ya nafsi zenu yakakudanganyeni. mpaka ilipo kuja amri ya Mwenyezi Mungu, na mdanganyifu akakudanganyeni msimfuate Mwenyezi Mungu.¹⁴

15. Basi leo haitapokelewa kwenu fidia, wala kwa wale walio kufuru. Makaazi yenu ni Motoni, ndio bora kwenu; na ni marejeo maovu yalioje!¹⁵

16. Je! Wakati haujafika bado kwa walio amini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyo teremka? Wala wasiwe kama walio pewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa wapotovu.¹⁶

yeyote mwenye chochote humo. Hawawi sawa kwa cheo na malipo kati yenu, mwenye kutoa kabla ya kutekwa Makka, na akapigana vita; na Uislamu unahitaji wa kuunga mkono na kuutilia nguvu. Hao walio toa na wakapigana kabla ya Ushindi wana cheo cha juu zaidi kuliko walio toa baada ya Ushindi (yaani kutekwa Makkah), na wakapigana. Na makundi yote mawili hayo Mwenyezi Mungu ameyaahidi kuwapa malipo mema juu ya kukhitalifiana vyeo vyao. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote myatendayo. Kwa hivyo atamlipa kila mmoja kwa anavyo stahiki.

11 Ni nani Muumini anaye toa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi, ili Mwenyezi Mungu apate kumlipa malipo yake mardufu, na tena juu ya hayo malipo mardufu apate malipo zaidi ya ukarimu Siku ya Kiyama?

12 Siku utapo waona Waumini wanaume na Waumini wanawake nuru ya Imani yao na vitendo vyao vizuri inawatangulia mbele yao na kuliani kwao. Malaika watawaambia: Furaha yenu hii leo ni kupata Bustani ambazo chini ya miti yake inapita mito. Hamtatoka humo kabisa. Malipo hayo ndiyo kufuzu kukubwa kwenu kulingana na vitendo vyenu.

13 Siku ambayo wanaafiki wanaume na wanaafiki wanawake watapo waambia Waumini wanaume na wanawake: Hebu tungojeeni tupate nasi baadhi ya nuru yenu. Wataambiwa kwa kuhiziwa: Rudini huko tuliko pewa nuru hii mkatake huko. Basi baina ya Waumini na wanaafiki utasimamishwa ukuta wenye mlango. Ndani ya ukuta upande wa Bustani itakuwapo rehema na neema. Na nje ya ukuta kunako elekea Motoni upande huo kutakuwa na nakama na adhabu.

14 Wanaafiki watawaita Waumini: Kwani duniani hatukuwa pamoja nanyi nasi ni wenzenu? Waumini waseme: Kwani! Mlikuwa kweli pamoja nasi, kama msemavyo. Lakini nyinyi mmejiangamiza wenyewe kwa anaafiki, na mkawa mnatamani Waumini yawapate masaibu ya kuwaangamiza, na mkatilia shaka mambo yote ya dini. Na tamaa mbovu zikakukhadaini ya kwamba nyinyi mko katika neema, mpaka yakaja mauti, na Shetani akakukhadaini kuwa bado mtapata msamaha kwa Mwenyezi Mungu na maghfira yake. (Ghururi hiyo wanayo wanaafiki wengi walio dhulumu watu na wakajidhulumu nafsi zao, wakawa wanadhani watasamehewa udhaalimu wao kwa kusali kwingi na kuhiji, bila ya kujirekibisha nafsi zao na kurejesha haki za walio wadhulumu.)

15 Basi leo hakitapokelewa chochote mtacho toa (enyi wanaafiki) kuwa ni fidia ya kujikombolea nafsi zenu na adhabu, hata ikiwa kwa thamani gani! Wala hakitapokelewa kitu kutokana na makafiri wenye kutangaza ukafiri wao kuwa ni fidia kadhaalika. Marejeo yenu nyote ni Motoni, na hayo ndiyo makaazi yenu yalio bora kwenu mnayo stahiki. Na uovu ulioje wa marejeo hayo!

16 Je! Haujafika wakati kwa walio amini zikalainika nyoyo zao kwa kumdhukuru Mwenyezi Mungu na

17. Jueni kwamba Mwenyezi Mungu huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Tumekubainishieni Ishara ili mpate kuzingatia.¹⁷
18. Kwa hakika wanaume wanao toa sadaka, na wanawake wanao toa sadaka, na wakamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, watazidishiwa mardufu na watapata malipo ya ukarimu.¹⁸
19. Na walio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, hao ndio Masidiqi na Mashahidi mbele ya Mola wao Mlezi. Wao watapata malipo yao na nuru yao. Na walio kufuru na wakakadhibisha Ishara zetu, hao ndio watu wa Motoni.¹⁹
20. Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na pumbao, na pambo, na kujifakhirisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake, kisha hunyauka ukayaona yamepiga manjano kisha yakawa mabua. Na akhera kuna adhabu kali na maghfira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu.²⁰
21. Kimbilieni msamaha wa Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi, iliyo wekewa walio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake. Hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu.²¹
22. Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika

Qur'ani tukufu, wala wasiwe kama walio pewa Kitabu kabla yao, Mayahudi na Wakristo. Walitenda kwa mujibu wa Kitabu kwa muda, lakini kwa kupita zama ndefu zikawa ngumu nyoyo zao, na wengi wao wakawa wametoka katika mipaka ya dini yao.

17 Enyi Waumini! Jueni kwamba Mwenyezi Mungu anaitengeneza ardhi na kuifanya isilihi kwa mimea kwa kuteremsha mvua baada ya kuyabisika kwake. Na Sisi tumekuwekeeni wazi Ishara na tumekupigieni mifano ili mpate kuzingatia katika hayo, na zinyenyekee nyoyo zenu kwa ajili ya kumdhukuru Mwenyezi Mungu.

18 Hakika wanaume wanao toa sadaka, na wanawake wanao toa sadaka, na wakatoa katika *Sabilillahi*, Njia ya Mwenyezi Mungu kwa ridhaa ya nafsi zao, Mwenyezi Mungu atawazidishia thawabu zao mara mbili, na wao juu ya kuzidishiwa kwao huko watapata ujira wa takrima Siku ya Kiyama.

19 Na walio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, wala wasibague baina yao yeyote, hao ndio Masidiqi (walio timia ukweli wao, kama Sayyidna Abubakar na Bibi Maryam), na Mashahidi (walio kufa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu) kwa cheo na utukufu wa daraja. Siku ya Kiyama watakuwa na thawabu na nuru kama thawabu na nuru za Masidiqi na Mashahidi. Na ambao wamekufuru na wakakadhibisha Ishara za Mwenyezi Mungu, hao ndio watu wa Motoni, na wala hawatoki humo milele.

20 Enyi mlio danganyika na dunia! Jueni kuwa uhai wa dunia ni mchezo usio leta faida, na pumbao la kumshughulisha mtu na yanayo mfaa, na pambo lisio mleta utukufu wa maana, na kujitapa baina yenu kwa nasaba zenye kuondoka, na mafupa yanayo oza, na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Mfano wa hayo ni kama mfano wa mvua inayo wafurahisha wakulima kwa mimea yake; kisha ikisha pevuka na kuiva, utaiona imegeuka manjano kwa kunyauka kwa ukame. Kisha mara yanakuwa mabua makavu yanakatika katika. Hakibakii chochote chenye manufaa. Na Akhera ipo adhabu kali kwa mwenye kuikhiari dunia na akaishika kwa isiyo kuwa haki yake. Na pia yapo maghfira ya Mwenyezi Mungu kwa mwenye kukhiari Akhera yake kuliko dunia yake. Na uhai wa dunia si chochote ila starehe ya udanganyifu isiyo ya kweli kwa mwenye tumaini nayo na asiifanye kuwa ni njia tu ya kutengenezea Akhera.

21 Nendeni upesi upesi kushindania kupata maghfira kwa Mola wenu Mlezi, na kwendea Pepo ilio enea kotekote, upana wake kama upana wa mbingu na ardhi, walio andaliwa wenye kumsadiki Mwenyezi Mungu na Mitume wake. Malipo hayo makubwa ni fadhila ya Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye katika waja wake. Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye fadhila iliyo tukuka hata akili haziwezi kuelezea.

Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.²²

23. Ili msihuzunike kwa kilicho kupoteeni, wala msijitape kwa alichu kupeni. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna akajifakhirisha.²³

24. Ambao wanafanya ubakhili, na wanaamrisha watu wafanye ubakhili. Na anaye geuka, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha, Msifiwa.²⁴

25. Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu, na tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu, na ili Mwenyezi Mungu amjue anaye mnusuru Yeye na Mitume wake kwa ghaibu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda.²⁵

26. Na bila ya shaka tulimtuma Nuhu na Ibrahim, na tukaweka katika dhuriya zao Unabii na Kitabu. Basi wapo miongoni mwao walio ongoka, na wengi katika wao ni wapotovu.²⁶

27. Tena tukafuatisha nyuma yao Mitume wengine, na tukamfuatisha Isa bin Mariamu, na tukampa Injili. Na tukajaalia katika nyoyo za walio mfuata upole na rehema. Na umonaki (utawa wa mapadri) wameuzua wao. Sisi hatukuwaandikia hayo, ila kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuufuata inavyo takiwa kuufuata. Basi wale walio amini katika wao tuliwapa ujira wao. Na wengi wao ni wapotovu.²⁷

28. Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na muaminini Mtume wake, atakupeni

22 Haukuteremka msiba wowote duniani, ikiwa ni ukame, au upungufu wa mazao, au mengineyo; wala katika nafsi zenu, ikiwa kwa maradhi, au ufakiri, au mauti au mengineyo, ila huwa yamekwisha andikwa katika *Lauhul Mahfudh*, Ubao Ulio hifadhiwa, na yamethibiti katika ujuzi wake Mwenyezi Mungu kabla ya kutokeza duniani au katika nafsi zenu. Hakika kuthibitishwa misiba na kujua ni mambo mepesi kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa ujuzi wake umeenea kila kitu.

23 Tumekujuyveni hayo ili msihuzunike kwa mnyao kuwa hamyapati kwa huzuni ya kupita kiasi hata ikatutieni uchungu, wala msifurahie kwa furaha ya kujitapa kwa anacho kupeni. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna na akajifakhiri juu ya watu kwa alichu nacho.

24 Wale wanao fanya choyo na mali yao wasitoe katika *Sabilillahi*, Njia ya Mwenyezi Mungu, na wanawaamrisha watu wafanye ubakhili ati kwa kuwa ndio wanawafanyia hisani; na mwenye kuacha kumt'ii Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu mwenyewe hamhitaji huyo, naye ni Mwenye kustahiki kuhimidiwa na kusifiwa.

25 Hakika tumewatuma Mitume wetu tulio wachagua kwa miujiza ya kukata, na tukateremsha pamoja nao Kitabu chenye kukusanya hukumu na sharia za Dini, na Mizani ya kuhakikisha insafu katika kuamiliana, ili watu wapate kuamiliana baina yao kwa uadilifu. Na tumekiumba chuma ambacho kina mateso makali katika vita, na manufaa kwa watu katika amani. Wanakitumia katika ufundi ili kiwanufaishe katika maslaha yao na maisha yao. Na ili Mwenyezi Mungu amjue anaye isaidia Dini yake, na anaye wasaidia Mitume wake kwa ghaibu, bila ya kuwaona. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenyewe Muweza, hamhitaji mtu kumsaidia. (*Tazama Maelezo 57:25*)

26 Na hakika tulimtuma Nuhu na Ibrahimu, na tukajaalia miongoni mwa vizazi vyao Unabii na Kitabu cha uwongofu. Basi baadhi ya wazao hao wapo walio fuata njia ya uwongofu, na wengi wao wametokana na Njia Iliyo Nyooka.

27 Kisha tukafuatiliza kwenye nyayo za Nuhu na Ibrahimu na walio watangulia hao au walio kuwa pamoja nao katika Mitume, Mtume baada ya Mtume, na tukafuatiliza kwa kumleta Isa mwana wa Mariamu. Na tukamfunulia Injili, na tukatia katika nyoyo za walio mfuata huruma nyingi, na upole, na rehema. Lakini kwa ziada katika ibada na kupita hadi katika kushika dini, wakazua Umonaki, ut'awa wa kujitenga na ulimwengu na kuacha kuoana. Sisi hatukawaamrisha hayo mwanzo. Lakini wao wameshika hayo kutafuta kumridhi Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini hawakuuhifadhi huo Umonaki kama inavyo stahiki kuhifadhiwa. Basi tukawapa walio muamini Muhammad sehemu yao ya ujira na thawabu. Na wengi wao wanamkadhifisha Muhammad, na wametoka nje ya ut'iifu na Njia Iliyo Nyooka. (*Tazama Maelezo 57:27*)

sehemu mbili katika rehema yake, na atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo. Na atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.²⁸

29. Ili watu wa Kitabu wajue kwamba wao hawana uweza wowote juu ya fadhila za Mwenyezi Mungu. Na fadhila zote zimo mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye fadhila kuu.²⁹

28 Enyi mlio amini, iogopeni adhabu ya Mwenyezi Mungu, na thibitini juu ya kumuamini kwenu Mtume wake. Mwenyezi Mungu atakupeni mafungu mawili katika rehema yake, na atakujaalieni muwe na nuru ya kukuongoeni, na atakusameheni yaliyo kuporonyokeni katika madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa maghfira, Mwenye rehema nyingi.

29 Mwenyezi Mungu anakupeni yote hayo ili wajue Watu wa Kitabu ambao hawakumuamini Muhammad ya kwamba hawana uweza wowote juu ya neema za Mwenyezi Mungu, wazipate wao au wampe mwenginewe. Na hakika fadhila zote zimo katika mikono ya Mwenyezi Mungu peke yake. Humpa amtakaye katika waja wake. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye fadhila kubwa.

Sura 58 - Al-Mujaadalah

Utangulizi

Sura imeanza kwa kueleza khabari za mwanamke anaye tengwa na mumewe, na ikafuatia kubainisha hukumu za kutengana. Na Mwenyezi Mungu katika sura hii katika zaidi ya Aya moja amewatia makosani wanao ifanyia uadui Dini yake, na amewahadharisha na kunong'ona nong'ona kwa ajili ya madhambi na uadui. Na amewaongoza Waumini juu ya adabu za kunong'ona baina yao kwa wao, na baina yao na Mtume s.a.w. Kama vile vile alivyo watia makosani wanaafiki kwa kushirikiana na makafiri, na akawaeleza kuwa hao ni kundi la Shetani lenye kuingia khasarani.

Na Sura ikakhitimisha kwa kueleza kwa jumla yaliyo ya waajibu juu ya Waumini ya kupendelea kumridhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake kuliko wengine wasio kuwa wao, hata wangeli kuwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Na akawasifu Waumini hao kuwa ni *Hizbu-Llahi*, Kundi la Mwenyezi Mungu, lenye kufanikiwa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. MWENYEZI MUNGU amekwisha sikia usemi wa mwanamke anaye jadiliana nawe juu ya mumewe, na anamshitakia Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anayasikia majibizano yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.¹

2. Wale miongoni mwenu wanao watenga wake zao, hao si mama zao. Hawakuwa mama zao ila wale walio wazaa. Na hakika hao wanasema neno linalo chusha, na la uwongo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kughufiria, Mwenye kusamehe.²

3. Na wale wanao jitenga na wake zao, kisha wakarudia katika yale waliyo yasema, basi wamkomboe mtumwa kabla hawajagusana. Mnapewa maonyo kwa hayo. Na Mwenyezi Mungu anayajua yote mnayo yatenda.³

4. Na asiye pata mtumwa kumkomboa, basi na afunge miezi miwili mfululizo kabla hawajagusana. Na asiye weza hayo basi awalishe masikini sitini. Hayo ni hivyo ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na kwa makafiri iko adhabu chungu.⁴

1 Mwenyezi Mungu amekwisha sikia kauli ya huyo mwanamke anaye kurejea wewe kwa shauri ya mumewe aliye jitenga naye kwa kudai ati anamwona kama mgongo wa mama yake, na akamlalamikia Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anayasikia hayo maneno mnayo jibizana. Hakika Mwenyezi Mungu anayasikia vyema yote ya kusikiwa, anayaona vyema yote ya kuonekana. (*Tazama Maelezo 58:1*)

2 Enyi Waumini! Hao miongoni mwenu wanao jitenga na wake zao kwa kuwashabihisha katika kuharimikiana nao kuwa ati ni kama mama zao, ni wakosa. Wake zao sio mama zao. Ukitaka haki mama zao ni wale walio wazaa tu. Na hakika wanao watenga wake zao kwa kusema hivyo wanasema kauli inayo chusha, inayo udhi katika murwa mwema, na ni uwongo ulio tokana na haki. Na hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mkuu wa kusamehe na kughufiria kwa yaliyo kwisha pita kwenu.

3 Na wale wanao watenga wake zao na kisha wakarejea kauli yao, wakayaona makosa yao, na wakataka kubaki na wake zao, basi juu yao kumkomboa mtumwa kabla ya kugusana. Hayo aliyo yawajibisha Mwenyezi Mungu, ya kukomboa mtumwa, ni mawaidha kwenu mnawaidhiwa ili msirejee tena katika makosa hayo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua vilivyo myatendayo.

4 Na asiye pata mtumwa wa kumkomboa, basi yampasa afunge miezi miwili mfululizo kabla hawajagusana.

5. Hakika wanao pinzana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, watadhalilishwa kama walivyo dhalilishwa wale walio kuwa kabla yao. Na tulikwisha teremsha Ishara zilizo wazi. Na makafiri watapata adhabu ya kufedhehesha.⁵
6. Siku atapo wafufua Mwenyezi Mungu, na awaambie yale waliyo yatenda. Mwenyezi Mungu ameyadhibiti, na wao wameyasahau! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushuhudia kila kitu.⁶
7. Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi? Hauwi mning'ono wa watu watatu ila Yeye huwa ni wane wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao. Wala wa wachache kuliko hao, wala walio wengi zaidi, ila Yeye yu pamoja nao popote pale walipo. Kisha Siku ya Kiyama atawaambia waliyo yatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.⁷
8. Kwani huwaoni wale walio katazwa kunong'onezana kisha wakayarudia yale yale waliyo katazwa, na wakanong'ona juu ya mambo ya dhambi, na ya uadui, na ya kumuasi Mtume? Na wakikujia hukuamkia sivyo anavyo kuamkia Mwenyezi Mungu. Na husema katika nafsi zao: Mbona Mwenyezi hatuadhibu kwa haya tuyasemayo? Basi Jahannamu itawatosha; wataingia humo! Na hayo ndiyo marejeo maovu yaliyoje!⁸
9. Enyi mlio amini! Mnapo nong'ona msinong'one kwa sababu ya mambo ya madhambi, na uadui, na kumuasi Mtume. Bali nong'onezane kwa kutenda mema na kuacha maovu. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwake mtakusanywa nyote.⁹
10. Kwa hakika minong'ono hiyo inatokana na Shetani ili awahuzunishe walio amini, na wala haitawadhuru chochote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na juu ya Mwenyezi Mungu tu ndio wategemeo Waumini.¹⁰

Na asiye weza kufunga hivyo basi itampasa awalisha masikini sitini. Tumeyalazimisha hayo ili mpace kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mtende kwa mujibu wa Imani hiyo. Na hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi msiikiuke. Na makafiri watapata adhabu yenye machungu makali.

5 Hakika wanao mfanyia inda Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kupingana nao watatupiliwa mbali kama walivyo tupiliwa mbali walio kuwa kabla yao. Na Sisi tumekwisha teremsha dalili zilizo wazi za kuonyesha Haki. Na hao wapinzani watapata adhabu ya kuwafedhehesha mno.

6 Siku Mwenyezi Mungu atapo wafufua wote baada ya kwisha kufa kwao, na awape khabari za yale waliyo yatenda. Mwenyezi Mungu amewawekea yote na ameyahifadhi, na wao wameyasahau. Na Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa yote na anayajua yote.

7 Kwani hujui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliomo mbinguni na yaliomo katika ardhi, na wala hapana siri ya watu watatu ila Yeye Mwenyezi Mungu ndiye wane wao kwa kuyajua kwake wanayo fanyia siri, wala hawawi watano ila na Yeye ndiye wa sita wao. Wala duni kuliko hivyo, wala kuzidi hivyo, ila Yeye yuko pamoja nao, anayajua hayo wanayo yanong'ona, popote walipo. Kisha Siku ya Kiyama atawapa khabari kwa kila walilo litenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kutimia ujuzi wake.

8 Ewe Mtume! Huwaoni hao walio katazwa kufanya njama za siri wao kwa wao kwa mambo ya kutia shaka katika nyoyo za Waumini, kisha wakayarejea yale yale waliyo katazwa? Na wanafanya njama kwa madhambi wanayo yatenda, na uadui wanao uazimia, na uasi dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na wanapo kuja kwako wanakuamkia kwa kauli ya kupotoa, sivyo anavyo kuamkia Mwenyezi Mungu. Na wao husema katika nafsi zao: Mbona Mwenyezi Mungu hatuadhibu kwa haya tunayo yasema ikiwa huyu ni Mtume kweli? Inawatosha hao Jahannamu. Wataingia humo waungue kwa moto wake. Na marejeo maovu yalioje marejeo yao. (*Tazama Maelezo 58:8*)

9 Enyi mlio msadiki Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Mnapo sema siri, basi msiwe mkisema siri katika mambo ya madhambi, na kufanya uadui, na kwenda kinyume na Mtume. Semeni siri katika mambo ya kheri, na kuepukana na madhambi. Na mwogopeni Mwenyezi Mungu ambaye kwake Yeye tu, si kwengineko, ndio mtakusanywa baada ya kufufuliwa.

10 Hakika kusema siri kwa kuchochea shaka shaka ni katika kuzainishwa na Shetani, ili apate kuingiza

- 11.** Enyi mlio amini! Mkiambiwa: Fanyeni nafasi katika mabaraza, basi fanyeni nafasi. Na Mwenyezi Mungu atakufanyieni nyinyi nafasi. Na mkiambiwa: Ondokeni, basi ondokeni. Mwenyezi Mungu atawainua walio amini miongoni mwenu, na walio pewa ilimu daraja za juu. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.¹¹
- 12.** Enyi mlio amini! Mnapo sema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu. Hiyo ni kheri kwenu na usafi zaidi. Na ikiwa hamkupata cha kutoa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.¹²
- 13.** Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu? Ikiwa hamkufanya hayo, na Mwenyezi Mungu akapokea toba yenu, basi shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.¹³
- 14.** Huwaoni wale walio fanya urafiki na watu ambao Mwenyezi Mungu amewakasirikia? Hao si katika nyinyi, wala si katika wao. Na huapa kwa uwongo, na hali kuwa wanajua.¹⁴
- 15.** Mwenyezi Mungu amewaandalia adhabu kali. Kwa hakika waliyo kuwa wakiyatenda ni maovu kabisa.¹⁵
- 16.** Wamefanya viapo vyao ni ngao, na wakaipinga Njia ya Mwenyezi Mungu. Basi hao watapata adhabu ya kufedhehesha.¹⁶
- 17.** Hayatawafaa kitu mali yao wala watoto wao mbele ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio watu wa Motoni. Humo watadumu milele.¹⁷
- 18.** Siku atakayo wafufua Mwenyezi Mungu wote, wamuwapie kama wanavyo kuwapieni nyinyi. Na watadhani kuwa wamepata kitu! Kwa hakika hao ndio waongo.¹⁸

huzoni katika nyoyo za Waumini. Wala hayo hayawezi kuwaletea madhara yoyote wao ila kwa kupenda Mwenyezi Mungu. Basi Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu peke yake..

11 Enyi mlio msadiki Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Mkitakiwa baadhi yenu kuwafanyia nafasi wenzenu mnapo kaa katika majlisi zenu, basi wafanyieni nafasi. Na Mwenyezi Mungu atakufanyieni nyinyi nafasi. Na mkitakiwa kuondoka pale mlipo kaa basi ondokeni. Mwenyezi Mungu hutukuza vyeo vya Waumini, na wale walio pewa ilimu kwa daraja nyingi. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.

12 Enyi mlio msadiki Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Mkitaka kusema siri na Mtume wa Mwenyezi Mungu, basi kabla ya mazungumzo yenu hayo tangulizeni kutoa sadaka. Hivyo ndio kheri yenu, na ni usafi zaidi kwa nyoyo zenu. Lakini ikiwa hamkupata cha kutoa sadaka, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa kusamehe, Mwenye kukusanya rehema zote.

13 Mnachelea kujilazimisha kutoa sadaka kabla ya mazungumzo yenu na Mtume wa Mwenyezi Mungu? Na ikiwa hamkutoa, na Mwenyezi Mungu akakusameheni, basi hifadhini kushika Sala na kutoa Zaka, na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za vitendo vyenu, naye atakulipeni kwavyo.

14 Ewe Mtume! Huwaoni wanaafiki walio wafanya marafiki watu ambao Mwenyezi Mungu ameghadhibika nao. Hawa wanao fanya urafiki si katika nyinyi, na hao wanao fanywa ni marafiki pia si katika nyinyi. Na wanaapa kwa uwongo, na huku wanajua kuwa wao ni waongo.

15 Mwenyezi Mungu amewatengenezea hawa wanaafiki adhabu ya mwisho wa ukali. Hakika vitendo vyao walivyo kuwa wakivitenda, vya unaafiki, na kuchukua viapo vya uwongo, ni viovu mno.

16 Wamefanya viapo vyao kuwa ndio viwe ni kinga ya kuwakinga wasiuliwe wenyewe, na watoto wao wasiwe mateka, na mali yao yasiwe ngawira. Kwa hayo wakaizuilia Njia ya Mwenyezi Mungu. Basi watapata adhabu ya fedheha.

17 Mali yao na watoto wao hayatawalinda na adhabu ya Mwenyezi Mungu hata chembe. Hao ni watu wa Motoni, wa kudumu humo milele.

18 Siku atapo wafufua Mwenyezi Mungu wote watamwapa kuwa hakika wao walikuwa ni Waumini, kama wanavyo kuapieni nyinyi hivi sasa. Na wanadhani kuwa kwa kuapa kwao huku ni ujanja utakao wafaa. Ama

19. Shetani amewatawala na akawasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hao ndio kundi la Shetani. Kweli hakika kundi la Shetani ndilo lenye kukhasirika.¹⁹

20. Hakika wanao mpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hao ndio miongoni mwa madhalili wa mwisho.²⁰

21. Mwenyezi Mungu ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.²¹

22. Huwakuti watu wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanao mpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao ameandika katika nyoyo zao Imani, na amewapa nguvu kwa Roho itokayo kwake. Na atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu awe radhi nao, na wao wawe radhi naye. Hao ndio *Hizbullahi*, Kundi la Mwenyezi Mungu. Hakika Kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufanikiwa.²²

kweli, hakika hawa wamefika ukomo wa uwongo!

19 Shetani amewatawala na amewasahaulisha kumdhukuru Mwenyezi Mungu na kuukumbuka utukufu wake. Hao ndio kundi la Shetani. Ama kweli, hakika kundi la Shetani ndilo lilio fikilia mwisho wa kukhasiri.

20 Hao wanao mfanyia inda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hao ndio katika hisabu ya walio fikilia ukomo wa udhalili.

21 Mwenyezi Mungu amekata hukumu: Bila ya shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu zilizo timia, hashindwi na yeyote.

22 Huwakuti watu wanao msadiki Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho wanapendana na wenye kumfanyia uadui Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hata wakiwa ni baba zao, au ni watoto wao, au ni ndugu zao, au ni jamaa zao. Hao ambao hawafanyi urafiki na wanao mpinga Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu ameithibitisha Imani katika nyoyo zao, na amewaunga mkono kwa nguvu zinazo tokana naye Yeye Mwenyewe, na atawatia katika Mabustani yapitayo mito kati yake wakikaa humo milele. Neema zake haziwakatikii. Mwenyezi Mungu amewapenda hao, na wao wamempenda. Hao ndio wanao ambiwa kuwa ni katika *Hizbullahi*, yaani Kundi la Mwenyezi Mungu. Hakika ni kweli Kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufuzu.

Sura 59 - Al-H'ashri

Utangulizi

Sura imeanzia kwa kutoa khabari kwamba kila kitu kilioko katika mbingu na ardhi kinamsabihi na kinamtakasa Mwenyezi Mungu na kila kitu ambacho si laiki naye. Na kwamba Yeye ni Mtukufu Mwenye nguvu asiye shindika, ni Mwenye hikima katika kuendesha kwake na kupanga kwake Sharia. Na katika matokeo ya nguvu zake na hikima yake ni yale yanayo simuliwa na Sura hii yaliyo wapata Bani Nnadhiri, nao ni katika Mayahudi wa Madina. Walikuwa hao walisuluhiana na Mtume s.a.w. baada ya kuhamia Madina kwamba wasiwe dhidi yake wala upande wake. Walipo shindwa Waislamu katika vita vya Uhud, walivunja agano lao wakaungana na Maqureshi dhidi ya Mtume s.a.w. Hapo ndipo akenda akwazunguka katika ngome zao ambazo walidhani wenyewe kuwa zitawalinda, na zisiweze kuwalinda. Tena ndio akawafukuza kutoka Madina. Kisha Sura inaeleza hukumu ya mali yaliyo patikana kwa maadui bila ya kupigana vita wala kukimbilia kwa farasi na kadhaalika. Ikataja kuwa hayo ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na jamaa, na mayatima, na masikini, na wasafiri, na mafakiri katika wakimbizi walio tolewa kwenye nyumba zao na mali yao. Kisha Sura ikasimulia khabari za Ansari, Waislamu wa Madina, na fadhila yao, na jinsi walivyo kuwa wanawafadhilisha Wahajiri, wakimbizi, kuliko nafsi zao, ijapo kuwa wao wenyewe wana haja ya hivyo wanavyo toa. Na Sura inataka macho yaangalie zile ahadi za wanaafiki kwa Bani Nnadhiri, na kauli yao waliyo sema: Pindi mkitolewa, nasi tutatoka pamoja nanyi! Na mkipigwa vita tutakusaidieni! Basi Sura imeufedhehi uwongo wao huo, udanganyifu wao katika hayo.

Kisha Sura ikamalizikia kwa kuwakumbusha Waumini kwa yatakianayo wawe nayo, nayo ni kumcha Mwenyezi Mungu, na kujiwekea akiba kwa siku zijazo za karibuni na za mbali. Na wala wasiwe kama wale walio mpuuzwa Mwenyezi Mungu, naye akawasahaulisha nafsi zao.

Na ikakhitimisha Sura kwa kubainisha hadhi ya Qur'ani na ubora wa taathira yake. Hayo ni hivyo kwa sababu aliye iteremsha ni Yeye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye Mwenye *Asmau-l-H'usna*, Majina Mazuri kabisa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Vinamsabihi, Vinamtakasa Mwenyezi Mungu viliomo katika mbingu na viliomo katika ardhi. Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹

2. Yeye ndiye aliye watoa walio kufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu katika nyumba zao wakati wa uhamisho wa kwanza. Hamkudhani kuwa watatoka, nao walidhani kuwa ngome zao zitawalinda na Mwenyezi Mungu. Lakini Mwenyezi Mungu aliwafikia kwa mahali wasipo patazamia, na akatia woga katika nyoyo zao. Wakawa wanazibomoa nyumba zao kwa mikono yao na mikono ya Waumini. Basi zingatieni enyi wenye

¹ Vitu vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi vinamtakasa Mwenyezi Mungu na kila lisio laiki naye. Na Yeye ndiye Mwenye kushinda ambaye hashindwi na kitu. Mwenye hikima katika mipango yake na vitendo vyake.

macho!²

3. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu asingeli waandikia kutoka, angeli waadhibu katika dunia. Na katika Akhera watapata adhabu ya Moto.³

4. Hayo ni kwa sababu walimpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mwenye kumpinga Mwenyezi Mungu, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.⁴

5. Mtende wowote mlio ukata au mlio uacha unasimama vile vile juu ya mashina yake, basi ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na kwa kuwahizi wapotovu.⁵

6. Na mali aliyo leta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwao hamkuyakimbilia mbio kwa farasi wala ngamia. Lakini Mwenyezi Mungu huwapa mamlaka Mitume wake juu ya wowote awatakao. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.⁶

7. Mali aliyo leta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa hivi vijiji ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na msafiri, ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu. Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.⁷

8. Wapewe mafakiri Wahajiri walio tolewa majumbani mwao na mali yao kwa ajili ya kutafuta fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi zake, na wanamsaidia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio wa kweli.⁸

9. Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda walio hamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyo pewa (Wahajiri), bali

2 Yeye Mwenyezi Mungu ndiye aliye watoa walio kufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu, nao ni Mayahudi wa ukoo wa Banu Nnadhira, kutoka kwenye majumba yao wakati wa kuwatoa mara ya kwanza katika Bara Arabu. Enyi Waislamu! Hamkudhania kuwa watatoka kwenye nyumba zao kwa sababu ya nguvu zao. Na wao wenyewe walidhani kwamba ngome zao zitawalinda na mashambulio ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu akawatokea katika upande wasio utarajia, na akawatia katika nyoyo zao fazaa kubwa, wakawa wanabomoa nyumba zao kwa mikono yao ili zibaki kuwa magofu tu, na kwa mikono ya Waumini wapate kuzivunja zile ngome. Basi enyi wenye akili, chukueni somo katika haya yaliyo washukia hawa.

3 Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hakuwahukumia kuwatoa majumbani kwao kwa sura hii ya kuchusha, basi hapana shaka angeli waadhibu katika dunia kwa shida zaidi kuliko huko kuwatoa. Na Akhera, wao watapata adhabu ya Moto, mbali huku kutolewa majumbani kwao duniani.

4 Hayo yaliyo wapata duniani na yanayo wangojea Akhera ni kwa sababu ya kuwa wamemfanyia uadui Mwenyezi Mungu na Mtume wake, uadui mkubwa mno. Na mwenye kumfanyia uadui Mwenyezi Mungu basi hawezi kupenya kuikimbilia adhabu yake. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

5 Enyi Waislamu! Mitende yoyote mliyo ikata au mkaiacha imebaki kama ilivyo kuwa, basi ni kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Hapana lawama juu yenu katika hayo, ili awape nguvu Waumini, na awahizi wapotovu walio ziacha sharia zake.

6 Na aliyo yaleta Mwenyezi Mungu na akayarudisha kwa Mtume wake katika mali ya Banu Nnadhira hamkuyapigia mbio nyinyi kwa farasi wala ngamia. Lakini Mwenyezi Mungu huwapa madaraka Mitume wake kwa awatakao katika waja wake bila ya kupigana vita. Na Mwenyezi Mungu ni Mtimilivu wa uweza juu ya kila kitu.

7 Alicho rudisha Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake katika mali ya watu wa vijiji hivi bila ya kuwatimua farasi au ngamia, vitu hivyo ni vya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na jamaa, na mayatima, na masikini, na wasafiri. Haya ni hivyo ili yasiwe mali yakizunguka katika mikono ya matajiri peke yao katika nyinyi. Na anacho kupeni Mtume katika hukumu basi kishikeni, na anacho kukatazeni basi kiwacheni. Na jilindeni na kughadhibika kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

8 Na hivyo yale mali ya watu wa vijiji aliyo yarudisha Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake wapewe mafakiri katika Wahajiri, walio kimbilia Madina, ambao wametolewa majumbani kwao na mali yao huko Makka. Wao wanataraji ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika riziki zao na radhi. Na wanamsaidia Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa nafsi zao na mali yao. Hao ndio Waumini wa kweli.

wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa.⁹

10. Na walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu.¹⁰

11. Huwaoni wanao fanya unaafiki wanawaambia ndugu zao walio kufuru katika Watu wa Kitabu: Mkitolewa na sisi lazima tutatoka pamoja nanyi, wala hatutamt'ii yeyote kabisa dhidi yenu. Na mkipigwa vita lazima tutakusaidieni. Na Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa hao hakika bila ya shaka ni waongo.¹¹

12. Pindi wakitolewa hawatatoka pamoja nao, na wakipigwa vita hawatawasaidia. Na kama wakiwasaidia basi watageuza migongo; kisha hawatanusuriwa.¹²

13. Hakika nyinyi ni kitisho zaidi katika vifua vyao kuliko Mwenyezi Mungu. Hayo ni kwa kuwa hao ni watu wasio fahamu kitu.¹³

14. Hawatapigana nanyi kwa mkusanyiko isipo kuwa katika vijiji vilivyo zatitiwa kwa ngome, au nyuma ya kuta. Wao kwa wao vita vyao ni vikali. Utawadhania kuwa wako pamoja, kumbe nyoyo zao ni mbali mbali. Hayo ni kwa kuwa wao ni watu wasio na akili.¹⁴

15. Ni kama mfano wa walio kuwa kabla yao hivi karibuni. Walionja uovu wa mambo yao. Nao watapata adhabu iliyo chungu.¹⁵

16. Ni kama mfano wa Shetani anapo mwambia mtu: Kufuru. Na akikufuru humwambia: Mimi si pamoja nawe. Hakika mimi namwogopa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.¹⁶

9 Na Ma-ansari, watu wa Madina walio mnusuru Mtume na Wahajiri, amba wamekaa Madina katika maskani zao, na Imani yao ikawa safi kabisa kabla ya kufika Wahajiri, wanawapenda wale wageni Waislamu walio hamia kwao, na wala hawahisi ubaya wowote katika nafsi zao kwa walicho pewa Wahajiri katika ngawira. Bali wanawakadimisha Wahajiri kuliko nafsi zao, ijapo kuwa wakiwa wao nao ni wahitaji. Na mwenye kuhifadhika, kwa uweza wa Mwenyezi Mungu, asione ubakhili katika nafsi yake, basi watu kama hao ndio wenye kufuzu kwa kila walipendalo.

10 Na Waumini walio kuja baada ya Wahajiri na Ansari husema: Mola wetu Mlezi! Tusamehe dhambi zetu, sisi na ndugu zetu walio tutangulia katika Imani. Wala usijaalie kuwa katika nyoyo zetu husda kuwahusudu walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe umefika ukomo katika upole na kurehemu.

11 Hebu huwaangalii hao wanaafiki ukastaajabu? Kazi yao ni kuwakariria kauli ndugu zao walio kufuru katika Watu wa Kitabu - nao ni hao Banu Nnadhiri - kuwaambia: Wallahi! Mkilazimishwa kuihama Madina, basi hapana shaka na sisi tutatoka pamoja nanyi. Wala hatutamt'ii katika jambo lenu mtu yeyote daima dawamu. Na pindi ikiwa Waislamu watakupigeni vita, basi hapana shaka sisi tutakusaidieni. Na Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa hakika wanaafiki hapana shaka ni waongo katika hizo ahadi zao wanazo zitoa.

12 Wakitolewa Mayahudi, wanaafiki hawatatoka pamoja nao. Na wakipigwa vita hawatawanusuru. Na pindi wakiwasaidia basi hapana shaka watatoka mbio warudi kinyume nyume, wala hawatawanusuru.

13 Hakika, enyi Waislamu, mna kitisho zaidi katika vifua vya wanaafiki na Mayahudi kuliko wanavyo mwogopa Mwenyezi Mungu. Hayo ni kwa sababu hakika wao ni watu wasio jua ukweli wa Imani.

14 Mayahudi hawapigani vita nanyi kwa pamoja ila wawe katika miji iliyo jengewa ngome, au wajifiche nyuma ya kuta. Vita vyao baina ya wao kwa wao ni vikali. Utawadhani kuwa wameshikamana, wote ni wamoja. Kumbe hakika nyoyo zao zimefarikiana mbali mbali. Wao ni wenye sifa hizo, kwa sababu hao ni watu wasio zingatia nini utakuwa mwisho wa mambo.

15 Mfano wa Bani Nnadhiri ni kama mfano wa walio kufuru kabla yao karibuni. Hao walionja hapa hapa duniani matokeo ya ukafiri wao na kuvunja kwao mapatano. Na Akhera watapata adhabu ya uchungu mkali.

16 Mfano wa wanaafiki kuwashawishi Banu Nnadhiri wamuasi Mtume wa Mwenyezi ni kama mfano wa

17. Basi ikawa mwisho wa wote wawili hao ni kuingia Motoni, wadumu humo daima; na hiyo ndiyo jaza ya madhaalimu.¹⁷
18. Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayo yatanguliza kwa ajili ya Kesho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari ya mnayo yatenda.¹⁸
19. Wala msiwe kama wale walio msahau Mwenyezi Mungu, na Yeye akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio wapotovu.¹⁹
20. Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.²⁰
21. Lau kuwa tumeiteremsha hii Qur'ani juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeli uona ukinyenyekea, ukipasuka kwa khofu ya Mwenyezi Mungu. Na hiyo mifano tunawapigia watu ili wafikiri.²¹
22. Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mwenye kuyajua yaliyo fichikana na yanayo onekana. Yeye ndiye Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.²²
23. Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake, Mwenye nguvu, Anaye fanya analo litaka, Mkubwa, Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayo mshirikisha nayo.²³
24. Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, Muumbaji, Mtengenezaji, Mtia sura, Mwenye majina mazuri kabisa. Kila kilioko katika mbingu na ardhi kinamtakasa, naye ni Mwenye kushinda, Mwenye hikima.²⁴

Shetani pale anapo mghuri mtu aiache Imani, akamwambia: Kufuru! Na alipo kufuru akasema: Mimi niko mbali nawe, kwani mimi ninamkhofu Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.

17 Ikawa basi marejeo ya Shetani na huyo anaye mzaini ni kuishia Motoni wabaki humo milele. Na kudumu humo dawamu ni malipo ya wenye kuasi wakaikiuka Njia ya Haki.

18 Enyi mlio amini! Jiwekeeni kinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kujilazimisha kumt'ii Yeye. Na kila nafsi izingatie a'mali gani ya kuikadimisha kwa ajili ya Kesho. Na jilazimisheni kumcha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari vilivyo kwa yote myatendayo. Naye atakulipeni kwa hayo.

19 Enyi Waumini! Msiwe kama wale walio sahu haki za Mwenyezi Mungu, na Yeye akawasahaulisha nafsi zao, kwa kuwajaribu kwa mitihani, na wakawa hawajui linalo wafaa na linalo wadhuru. Hao ndio walio toka wakaacha ut'iifu wa Mwenyezi Mungu.

20 Hawawi sawa watu wa Motoni wanao teswa, na watu wa Peponi wanao neemeshwa. Watu wa Peponi peke yao ndio wenye kufuzu kwa kila walipendalo.

21 Lau tungeli iteremsha hii Qur'ani juu ya mlima wenye nguvu basi ungeli uona huo mlima, juu ya nguvu zake, unanyenyekea na unapasuka kwa kumwogopa Mwenyezi Mungu. Na hiyo ni mifano tunawaeleza watu ili wapate kuzingatia matokeo ya mambo yao.

22 Yeye Mwenyezi Mungu ambaye hapana wa kuabudiwa kikweli isipo kuwa Yeye peke yake, Mwenye kujua lilio pita na lilioko sasa. Yeye ndiye Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.

23 Yeye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye, Mwenye kumiliki kila kitu kwa hakika, Aliye safika na kila upungufu, Aliye takasika na kila lisio mwelekea, Mwenye kusalimika na yote ya upungufu, Mwenye kuwaamini na kuwasadiki Mitume wake aliyi wapa nguvu kwa miujiza, Mlinzi Mwenye kuangalia kila kitu, Mwenye kushinda basi hashindwi na chochote, Mkubwa wa shani katika nguvu na utawala, Mwenye kutukuka na kila kisicho kuwa laiki na uzuri wake na utukufu wake, Mwenyezi Mungu ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo.

24 Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, Mwenye kuvumba vitu vyote tangu mwanzo bila ya ruwaza ya kuigia iliyo tangulia, Mwenye kuvipa sura kama vilivyo kwa mujibu wa atakavyo Yeye. Yeye ndiye Mwenye Majina Mazuri, Mwenye kutakaswa na kila kisicho kuwa laiki yake na kila kilichoko katika mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye kushinda, asiye shindwa na kitu. Mwenye hikima katika kupanga kwake na sharia zake.

Sura 60 - Al-Mumtah'inah

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kuwakataza Waumini wasiwafanye urafiki washirikina, ambao ni maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zao wao, kwa kushikilia kwao ukafiri, na kumtoa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Waumini kwenye nyumba zao Makka. Na ikaashiria kwamba uadui wa watu hawa kwa Waumini, ulio fichikana, hauwachi kudhihiri pale wanapo wakuta na wakapata nguvu juu yao.

Kisha Sura ikaingia kubainisha ruwaza njema ya Ibrahim na walio kuwa pamoja naye katika kujitenga na washirikina, na hayo waliyo kuwa wakiyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu, wakitangaza uadui wao kwao mpaka wamuamini Mwenyezi Mungu peke yake. Hayo yanaonyesha kuwa huo ndio mwendo wa wanao taraji kukutana na Mwenyezi Mungu, na wanaogopa adhabu yake.

Kisha ikabainisha makhusiano yepi yanafaa kuwa nayo na wasio kuwa Waislamu, na yepi hayafai. Ama wale ambao hawatupigi vita katika Dini wala hawasaidii dhidi yetu, basi ni waajibu wetu kuwafanyia wema, na kuwafanyia haki. Ama hao wanao tupiga vita katika Dini, na wakasaidia katika kututoa kwenye nyumba zetu na miji yetu, hao, basi, ndio Mwenyezi Mungu anatakataza kuwafanyia hisani na kukhusiana nao.

Kisha Sura ikabainisha hukumu ya Waumini wanawake walio hamia kwenye mji wa Kiislamu, na wakawaacha waume zao wa kishirikina; na hukumu ya wanawake wa kishirikina ambao waume zao Waislamu wamehama, na hao wanawake wakaachwa katika mji wa shirki.

Na ikafuatiliza kueleza kutoa ut'iifu wanawake, kwa walivyo mtolea Mtume s.a.w. Kisha Sura ikakhitimisha, kama ilivyo anza, kwa kukataza kuwafanya urafiki maadui walio kasirikiwa na Mwenyezi Mungu, ili kuthibitisha hukumu iliyo kwisha tolewa mwanzo wake, na ikaitilia nguvu katika kuthibitisha kwake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Enyi mlio amini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi, na hali wao wamekwisha ikataa haki iliyo kujieni, wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu. Mnapotoka kwa ajili ya Jihadi katika Njia yangu na kutafuta radhi yangu, mnaifanya urafiki nao kwa siri, na Mimi nayajua mnayo yaficha na mnayo dhihirisha. Na mwenye kufanya hayo kati yenu basi ameipotea njia ya sawa.¹

2. Wakikuwezeni wanakuwa maadui zenu, na wanakukunjulieni mikono yao na ndimi

¹ Enyi mlio msadiki Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Msiwafanye maadui wangu na maadui wenu kuwa ni wenzenu mkiwapa mapenzi ya kweli, na hali wao wameyakataa yaliyo kujieni nyinyi ya kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Kitabu chake. Wamemtoa Mtume na wamekutoeni nyinyi kwenu kwenye majumba yenu, kwa sababu ya Imani yenu kumuamini Mwenyezi Mungu, Mola wenu Mlezi. Mnapotoka makwenu kwenda pigana Jihadi katika Njia yangu na kutaka radhi yangu, basi msifanye urafiki na adui zangu, mkawapa mapenzi kisirisiri. Na Mimi nayajua vyema yote mnayo yaficha na mnayo dhihirisha. Na yeyote mwenye kumfanya adui wa Mwenyezi Mungu kuwa ndiye rafiki yake basi ameikosea Njia Iliyo Nyooka.

zao kwa uovu. Na wanapenda muwe makafiri.²

3. Hawatakufaeni jamaa zenu, wala watoto wenu Siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu atapambanua baina yenu, na Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yatenda.³

4. Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale walio kuwa pamoja naye, walipo waambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni; na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka mtakapo muamini Mwenyezi Mungu peke yake. Isipo kuwa kauli ya Ibrahim kumwambia baba yake: Hakika nitakuombea msamaha, wala similiki chochote kwa ajili yako mbele ya Mwenyezi Mungu. Mola wetu Mlezi! Juu yako tumetegemea, na kwako tumeelekea, na kwako ndio marejeo.⁴

5. Mola wetu Mlezi! Usitufanyie mtihani kwa walio kufuru. Na tusamehe, Mola wetu Mlezi. Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.⁵

6. Kwa yakini umekuwa mfano mzuri kwenu katika mwendo wao, kwa anaye mtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na mwenye kugeuka basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosa, Msifiwa.⁶

7. Asaa Mwenyezi Mungu akatia mapenzi baina yenu na hao maadui zenu, na Mwenyezi Mungu ni Mweza, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.⁷

8. Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.⁸

2 Wakikutana nanyi na wakakuwezeni, uadui wao kwenu unadhihiri, na wanakunyoo sheeni mikono yao na ndimi zao kukudhuruni. Na wanatamani muwe makafiri kama wao.

3 Hawatakufaeni kitu jamaa zenu wala watoto wenu mlio wafanya kuwa ni marafiki, na hali wao ni adui wa Mwenyezi Mungu na adui zenu. Katika Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atakutengeni mbali mbali. Atawatia maadui zake Motoni na marafiki zake Peponi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona yote myatendayo.

4 Nyinyi mna kiigizo kizuri cha kukiiga katika Ibrahim na walio amini pamoja naye, pale walipo waambia watu wao: Hakika sisi tunajitenga nanyi, na tunajitenga na hiyo miungu ya uwongo mnayo iabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Sisi tunakukataeni, na umekwisha dhihiri uadui na kuchukiana baina yetu na nyinyi. Hayo hayataondoka kabisa mpaka mumuamini Mwenyezi Mungu peke yake. Lakini kauli ya Ibrahim kumwambia baba yake: Nitakutakia maghfira, na similiki kwa Mwenyezi Mungu kitu chochote - kauli hiyo si ya kufuatwa. Kwani hayo yalikuwa kabla hajajua huyo baba yake kashikilia kuwa adui wa Mwenyezi Mungu wala hageuki. Ilipo dhihiri kwake kuwa hakika huyo ni adui wa Mwenyezi Mungu alijitenga naye. Enyi waumini! Semeni: Mola wetu Mlezi! Kwako Wewe ndio tunategemea, na kwako Wewe tunarejea, na kwako Wewe ndio mwisho wetu Akhera.

5 Mola wetu Mlezi! Usitujalie tukawa katika hali ya kuwa katika fitina za walio kufuru. Na tusamehe madhambi yetu, ewe Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu isiye shindika, Mwenye hikima katika kutasarafu kwake.

6 Enyi Waumini! Bila ya shaka katika Ibrahim na walio kuwa pamoja naye, kipo kiigizo kizuri kwenu kwa vile walivyo wafanyia uadui maadui wa Mwenyezi Mungu. Kiigizo hicho ni kwa mwenye kutaraji kukutana na Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na mwenye kupuuzwa kufuata haya basi kajidhulumu nafsi yake. Kwani hakika Mwenyezi Mungu si mhitaji wa mwengine. Yeye ni Mwenye kustahiki peke yake sifa zote njema.

7 Asaa Mwenyezi Mungu akajaalia yawepo mapenzi baina yenu na hao makafiri walio ni maadui zenu, kwa kuwapa tawfikii, kuwawezesha, kuingia katika Imani. Na Mwenyezi Mungu ana uweza ulio timia, ni Mkunjufu wa maghfira kwa mwenye kutubu, ni Mwenye kuwarehemu waja wake.

8 Mwenyezi Mungu hakukatazini kwa makafiri wasio kupigeni vita wala kukufukuzeni makwenu kuwakirimu na kuwapa mawasiliano mema. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda watu watendao

9. Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale walio kupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanao wafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu.⁹

10. Enyi mlio amini! Wakikujilieni wanawake Waumini walio hama, basi wafanyieni mtihani - Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua zaidi Imani yao. Mkiwa mnawajua kuwa ni Waumini basi msiwarudishe kwa makafiri. Wanawake hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalaliki wanawake Waumini. Na wapeni hao wanaume mahari walio toa. Wala hapana makosa kwenu kuwaoa mkiwapa mahari yao. Wala msiwaweke wanawake makafiri katika kifungo cha ndoa zenu. Na takeni mlichokitoa, na wao watake walichokitoa. Hiyo ndiyo hukumu ya Mwenyezi Mungu anayo kuhukumuni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima.¹⁰

11. Na akitoroka yeyote katika wake zenu kwenda kwa makafiri, tena ikatokea mkapata ngawira, basi wapeni walio kimbiwa na wake zao kiasi cha mahari waliyo yatoa. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mnamuamini.¹¹

12. Ewe Nabii! Watakapo kujia wanawake Waumini wanakuahidi ya kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawauwa watoto wao, wala hawataleta uzushi wanao uzua tu wenyewe baina ya mikono yao na miguu yao, wala hawatakuasi katika jambo jema, basi peana nao ahadi, na uwatakie maghfira kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi maghfira, Mwenye kurehemu.¹²

ihsani na mawasiliano.

9 Ila Mwenyezi Mungu anakukatazeni wale walio kupigeni vita katika Dini ili kukuzieni nayo, na wakakulazimisheni kutoka majumbani kwenu na nchi yenu, na wakasaidia katika kukutoeni huko, msiwafanye hao kuwa ndio wenzenu wa kusaidiana nao. Na wenye kuwafanya hao ndio wasaidizi wao, basi hao ndio wenye kujidhulumu nafsi zao.

10 Enyi mlio amini! Wakikujieni wanawake Waumini walio hama kukimbia nchi ya ukafiri, basi wachungueni ili mpate kujua ukweli wa Imani yao. Mwenyezi Mungu anajua zaidi ukweli wa Imani yao. Mkiwaona kama ni Waumini, basi msiwarudishe kwa waume zao makafiri. Wanawake Waumini si halali kwa makafiri, wala wanaume makafiri si halali kwa wanawake Waumini. Na wapeni waume wa kikafiri mahari waliyo yatoa kwa wake zao walio hamia kwenu. Wala hapana ubaya kwenu kuwaoa wanawake hao walio hamia kwenu mkiwapa mahari yao. Wala msiwazuie kwa kifungo cha ndoa wanawake makafiri walio bakia katika mji wa ukafiri au walio fungamana nao. Na takeni kwa makafiri mahari mliyo yatoa kwa wenye kufungamana na mji wa ukafiri. Na wao hao watake kulipwa walichokitoa kuwapa wake zao walio hama wakaja kwenu. Hukumu hiyo ni kwa mujibu wa sharia ya Mwenyezi Mungu, anayo kufafanulieni. Na Mwenyezi Mungu anajua vyema maslaha ya waja wake, ni Mwenye hikima katika kutoa sharia.

11 Na wakitokea baadhi ya wake zenu wakakukimbieni kwenda kwa makafiri, kisha mkapigana nao vita, basi wapeni walio kimbiwa na wake zao kiasi cha mahari waliyo yatoa. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mnamuamini.

12 Ewe Nabii! Wakikujia wanawake Waumini kukuahidi kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatwauwa watoto wao, wala hawatwabandikiza waume zao watoto wao (wa haramu) kwa uzushi na uwongo wanao uzua baina ya mikono yao na miguu yao. (yaani matumboni mwao, au kwa ndimi zao na tupu zao); wala hawendi kinyume nawe katika jambo jema unalo waitia, basi pokea ahadi zao juu ya hayo, na waombe msamaha kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe na kurehemu. (Mtume s.a.w. haamrishi ila jema, lakini sharia hapo inasema kuwa mtawala yeyote hut'iwa akiamrisha jema tu. Ama kwa lilio ovu, Mtume s.a.w. amesema: "Hapana kumtii kiumbe katika kumuasi Muumba.")

13. Enyi mlio amini! Msiwafanye rafiki zenu watu ambao Mwenyezi Mungu amewakasirikia. Hao wamekwisha kata tamaa ya Akhera, kama makafiri walivyo wakatia tamaa watu wa makaburini.¹³

13 Enyi mlio msadiki Mwenyezi Mungu na Mtume wake, msiwafanye kuwa rafiki zenu watu ambao Mwenyezi Mungu amewaghadhibikia. Hao wamekata tamaa na Akhera na yote yatakao kuwapo huko, ya kulipwa na kuhisabiwa, kama makafiri walivyo kata tamaa kufufuliwa waliomo makaburini.

Sura 61 - Ass'af

Utangulizi

Sura hii imefunguka kwa kutoa khabari kwamba viliomo katika mbingu na katika ardhi vinamsabihi Mwenyezi Mungu. Na kwamba haiwaelekei Waumini kusema wasiyo yatenda. Na hakika Mwenyezi Mungu anapenda wawe mkono mmoja. Kisha Sura imewashutumu Wana wa Israili kuwa ni wenye inda na ukafiri kwa kauli za Mitume wawili watukufu, nao ni Musa na Isa s.a.w. Na kwamba wao wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuitimiza nuru yake. Na ndani ya hii Sura ipo ahadi ya Mwenyezi Mungu - na ahadi yake ni ya kweli - kuwa ataifanya Dini hii ishinde dini zote nyenginezo, hata walau washirikina wakichukia. Na ikakhitimishia kwa kuhimiza Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa hali na mali, na kuwaahidi wenye kupigana Jihadi, Mujahidina, kupata msamaha na Pepo, na mengineyo wayapendayo Waumini, nayo ni msaada utokao kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi wa karibu. Na wanahimizwa Waumini wawe wenye kumsaidia Mwenyezi Mungu, kama walivyo kuwa wanafunzi wa Isa bin Mariamu. Na kwamba Mwenyezi Mungu atawaunga mkono Waumini kwa msaada wake, na Yeye ni Mwenye kushinda katika kila kitu, Mwenye hikima ya ukomo.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Vinamtakasa Mwenyezi Mungu viliomo katika mbingu na katika ardhi. Na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹
2. Enyi mlio amini! Kwa nini mnasema msiyo yatenda?²
3. Yanachukiza vikubwa mno kwa Mwenyezi Mungu kuwa mnasema msiyo yatenda.³
4. Kwa hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao pigana katika Njia yake kwa safu kama jengo lilio kamatana.⁴
5. Na Musa alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Kwa nini mnaniudhi, nanyi mnajua kuwa hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu niliye tumwa kwenu? Walipo potoka, Mwenyezi Mungu aliziachia nyoyo zao zipotoke. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu.⁵
6. Na Isa bin Mariamu alipo sema: Enyi Wana wa Israili! Hakika mimi ni Mtume wa

1 Kila kiliomo katika mbingu na kiliomo katika ardhi kinamtakasa Mwenyezi Mungu na kila kisicho kuwa ni laiki yake. Na Yeye peke yake ndiye Mwenye kuvishinda vitu vyote, Mwenye hikima iliyo fika ukomo.

2 Enyi mlio amini! Kwa ajili ya nini mnasema kwa ndimi zenu yasiyo hakikishwa na vitendo vyenu?

3 Mwenyezi Mungu anachukia mno kuwa nyinyi mnasema msiyo yatenda.

4 Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao pigania kutaka kulinyanyua Neno lake nao wameshikamana kitu kimoja, kama kwamba wao ni jengo lilio simama imara.

5 Ewe Muhammad! Kumbuka pale Musa alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Kwa nini mnaniudhi mimi, na hali nyinyi mnajua kwamba hakika mimi ni Mjumbe niliye tumwa na Mwenyezi Mungu nije kwenu? Walipo endelea na kuiacha Haki, Mwenyezi Mungu alizipotoka nyoyo zao zisipokee uwongofu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu walio toka kwenye ut'ifu wake.

Mwenyezi Mungu kwenu, ninaye thibitisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakaye kuja baada yangu; jina lake ni Ahmad! Lakini alipo waletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi ulio dhaahiri!⁶

7. Na ni nani mwenye kudhulumu zaidi kuliko yule anaye mzulia Mwenyezi Mungu uwongo, naye anaitwa kwenye Uislamu? Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.⁷

8. Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapo kuwa makafiri watachukia.⁸

9. Yeye ndiye aliye mtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya haki ili ipate kuzishinda dini zote, ijapo kuwa washirikina watachukia.⁹

10. Enyi mlio amini! Nikuonyesheni biashara itakayo kuokoeni na adhabu iliyo chungu?¹⁰

11. Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganeni Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu, ikiwa nyinyi mnajua.¹¹

12. Atakusameheni dhambi zenu, na atakutieni katika Mabustani yapitiwayo na mito kati yake, na maskani nzuri nzuri katika Bustani za milele. Huko ndio kufuzu kukubwa.¹²

13. Na kinginecho mkipendacho, nacho ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi ulio karibu! Na wabashirieni Waumini!¹³

14. Enyi mlio amini! Kuweni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu, kama alivyo sema Isa

6 Na kumbuka pale Isa bin Mariamu alipo sema: Enyi Wana wa Israili! Hakika mimi ni Mtume nimetumwa kwenu, mwenye kusadikisha yaliyo nitangulia yaliomo katika Taurati, na kukupeni bishara ya Mtume atakaye kuja baada yangu. Jina lake ni Ahmad. Alipo kuja huyo Mtume aliye bashiriwa kwa Ishara zilizo wazi wakasema: Haya uliyo tujia nayo ni uchawi dhaahiri!

(Kwa ushahidi wa kubashiriwa Nabii Muhammad s.a.w. katika vitabu vya Kikristo na Kiyahudi, tazama: Kumbukumbu la Torati 18.19-22, na Injili ya Yohana 16.5-14.)

7 Na nani aliye zidi kwa udhaalimu kuliko huyo aliye mzulia uwongo Mwenyezi Mungu, naye anaitwa aingie katika Dini ya Kiislamu, Dini ya haki na kheri? Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu walio shikilia dhulma.

8 Wana wa Israili wanamzulia Mwenyezi Mungu uwongo, ili ati wapate kuizima nuru ya Dini yake kwa vinywa vyao, kama anaye taka kuizima nuru ya jua kwa kuipulizia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuikamilisha nuru yake kwa kuitimiza Dini yake hata hao makafiri wakiudhika.

9 Mwenyezi Mungu ndiye aliye mtuma Mtume wake, Muhammad, pamoja na Qur'ani ambayo ni uwongofu kwa watu wote, na Uislamu ambao ndio Dini ya haki, ili autukuze juu ya dini zote, ijapo kuwa washirikina wataudhika.

10 Enyi mlio amini! Nikuongozeni kwenye biashara kubwa ambayo itakuokoeni na adhabu yenye machungu makali?

11 . Biashara hii ni kuwa mumuamini Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na mpigane Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu. Hayo aliyo kuonyesheni ndiyo kheri yenu ikiwa nyinyi mnajua.

12 Muamini na mpigane Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, ili akusameheni madhambi yenu, na akutieni katika Bustani zinazo pita kati yake mito, na maskani nzuri katika Bustani za milele. Hayo ndiyo malipo makubwa.

13 Na neema nyengine ambazo Waumini Mujahidina wanazo zipenda, ni msaada utokao kwa Mwenyezi Mungu na ushindi wa karibu utakao kuleteeni kheri zake. Na ewe Muhammad! Wabashirie Waumini kuwa watakata malipo haya.

Sura 61 - Ass'af

bin Mariamu kuwaambia wanafunzi wake: Nani wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu? Wakasema wanafunzi: Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu! Basi taifa moja la Wana wa Israili liliamini, na taifa jingine lilikufuru. Basi tukawaunga mkono walio amini dhidi ya maadui zao, wakawa wenye kushinda.¹⁴

14 Enyi mlio amini! Kuweni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu anapo kutakeni Mtume wa Mwenyezi Mungu muwe wasaidizi wake. Kama walivyo kuwa masahaba wa Isa wasaidizi wa Mwenyezi Mungu alipo sema: Nani wa kunisaidia mimi kwa Mwenyezi Mungu? Basi kundi moja katika Wana wa Israili lilimuamini Isa, na kundi jingine likamkataa. Sisi tukawapa nguvu walio amini juu ya maadui zao walio kufuru. Basi kwa kuwapa nguvu kwetu wakawa ni wenye kushinda.

Sura 62 - Al-Jumua'

Utangulizi

Imefunguka Sura hii kwa kutoa khabari yake Mtukufu kwamba viliomo katika mbingu na ardhi vyote vinamsabihi Yeye. Na Mwenyezi Mungu aliye tukuka shani yake amesema kwamba ameineemesha kaumu isio jua kuandika wala kusoma kwa kuwaletea Mtume miongoni mwao, ambaye anawafundisha Kitabu, na hikima, na anawatakasasa. Na hakika hii ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye.

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amewakemea Mayahudi kwa kuacha kwao kutenda yaliyo amrishwa katika Taurati, na hali wao wanajua yaliomo humo. Na amepinga madai yao kwamba wao peke yao ndio vipenzi vya Mwenyezi Mungu, si watu wengine. Na amebariziana nao kwa kuwataka watamani kufa ikiwa wao wanasema kweli! Na Sura imekhitimisha kwa kuwaamrisha Waumini wakimbilie kwenda sali Sala ya Ijumaa pindi wakisikia adhana, na waache biashara. Na Sala ikisha malizika watawanyike katika nchi wende kutafuta fadhila za Mwenyezi Mungu. Na kawakataza wasiache biashara au jambo la pumbao lolote kuwashughulisha wasiisikilize khutba ya Ijumaa. Na Mwenyezi Mungu amewadhamini kuwaruzuku, na Yeye ndiye mbora wa kuruzuku.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi vinamtakasa Mwenyezi Mungu, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹
2. Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye watu wasio jua kusoma, awesomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri.²
3. Na kwa wengine ambao bado hawajaungana nao. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.³
4. Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu anayo mpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa.⁴
5. Mfano wa walio bebeshwa Taurati kisha wasiibebe, ni mfano wa punda anaye beba

1 Vitu vyote viliomo katika mbingu na viliomo katika ardhi vinamsabihi na kumtakasa Mwenyezi Mungu na kila kisicho kuwa laiki, Yeye ndiye Mfalme wa kila kitu, Mwenye kuendesha atakavyo bila ya mpinzani, Mwenye kutakasika kwa ukamilifu na kila cha upungufu, Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye hikima ya kufika mwisho.

2 Mwenyezi Mungu ndiye aliye mtuma Mtume kwa watu wasio jua kuandika, naye ni katika wao wenyewe, anawasomea Aya zake Mwenyezi Mungu, na anawasafisha na mambo machafu ya itikadi na tabia, na anawafundisha Qur'ani na kuijua Dini. Na wao kabla ya kuletwa yeye walikuwa wamepotoka kabisa kuiacha haki.

3 Na pia Mwenyezi Mungu amempeleka Muhammad kwa watu wengine, ambao hawajaja bado, lakini watakuja. Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye Mwenye kushinda kila kitu, Mwenye hikima ya kufikia ukomo katika vitendo vyake.

4 Kuletwa Mtume huko ni fadhila inayo toka kwa Mwenyezi Mungu. Anamkirimu kwayo aliye mkhitari katika waja wake. Na Mwenyezi Mungu peke yake, ndiye Mwenye fadhila kubwa.

vitabu vikubwa vikubwa. Mfano muovu mno wa watu walio kadhibisha Ishara za Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhaalimu.⁵

6. Sema: Enyi mlio Mayahudi! Ikiwa nyinyi mnadai kuwa ni vipenzi vya Mwenyezi Mungu pasipo kuwa watu wengine, basi yatamanini mauti, ikiwa mnasema kweli.⁶

7. Wala hawatayatamani kabisa, kwa sababu ya iliyo kwisha yatanguliza mikono yao. Na Mwenyezi Mungu anawajua walio dhulumu.⁷

8. Sema: Hayo mauti mnayo yakimbia, bila ya shaka yatakukuteni. Kisha mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu yaliyo fichikana na yanayo onekana. Hapo atakwambieni mliyo kuwa mkiyatenda.⁸

9. Enyi mlio amini! Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua.⁹

10. Na itakapo kwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa.¹⁰

11. Na wanapo iona biashara au pumbao wanayakimbilia hayo na wakakuacha umesimama. Sema: Yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko pumbao na biashara. Na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa watoa riziki.¹¹

5 Mfano wa Mayahudi walio funzwa Taurati, na wakalazimishwa waifuata, na wao hawakuifuata kwa vitendo, ni mfano wa punda aliye beba vitabu ambavyo hajui ndani yake mna nini. Ni mbaya mno mfano wa watu wanao kadhibisha Ishara za Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hawasaidii kufikilia uwongofu watu ambao kazi yao ni kudhulumu.

6 Ewe Muhammad! Sema: Enyi nyinyi mlio Mayahudi! Kama mnadai kwa uwongo kwamba nyinyi peke yenu ati ndio vipenzi vya Mwenyezi Mungu, basi takeni mauti kwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnasema kweli katika hayo madai ya kwamba Mwenyezi Mungu anakupendeni.

7 Mwenyezi Mungu anasema: Wala Mayahudi hawatamani mauti milele kwa sababu ya ukafiri na vitendo viovu walio kwisha vitenda. Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema walio dhulumu.

8 Sema: Hayo mauti mnayo yakimbia hamwezi kuyakimbia, bila ya shaka yatakukuteni tu. Kisha mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu kujua ya siri na ya dhaahiri. Na Yeye atakwambieni mliyo kuwa mkiyatenda.

9 Enyi mlio amini! Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa, basi nendeni kwa hima na hamu kumkumbuka na kumtaja Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo mliyo amrishwa yana nafuu zaidi kwenu nyinyi, ikiwa mnajua.

10 Mkisha maliza kusali basi tawanyikeni katika nchi kwa ajili ya maslaha yenu, na mtake fadhila za Mwenyezi Mungu. Na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa nyoyo zenu na ndimi zenu kwa wingi, ili asaa mkafuzu katika kheri za duniani na Akhera.

11 Na wakiona bidhaa za biashara, au pumbao lolote hutawanyika kuendea hayo, na wakakuacha wewe umesimama unakhutubu! Waambie: Fadhila na thawabu zilioko kwa Mwenyezi Mungu zina nafuu zaidi kwenu kuliko pumbao na kuliko biashara. Na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa wanao toa riziki. Basi itafuteni riziki yake kwa kumt'ii Yeye.

Sura 63 - Al-Munaafiqun

Utangulizi

Sura hii imekusanya kikundi cha sifa za wanaafiki; ikataja kwamba hao hutangaza imani yao kwa ndimi zao bila ya kuwa wanasema kweli. Na ikabainisha kwamba wanafanya yamini zao za uwongo kuwa ni kinga wasiambiwe kuwa ni makafiri, ambao kwa hakika ndivyo walivyo na ndivyo watakatavyo lipwa hivyo. Pia imebainisha kuwa hao wanaafiki wana umbo zuri la kumpendeza anao waona, na wana ufasihi mzuri wa kusikilizwa. Na juu ya hivyo, nyoyo zao zi tupu, hazina Imani ndani yake. Wao ni kama magogo yaliyo egemezwa, yasiyo na uhai.

Na Sura inaelezea kuwa wakiitwa ili Mtume wa Mwenyezi Mungu awaombee maghfiira, hali yao hubainika kwa kuwa hutakabari, na hudhihirisha kukataa kwao kuitikia, nao wanajivuna.

Kisha Sura ikaingia kutaja madai ya wanaafiki kwamba wao ati ndio watukufu wenye nguvu, na Waumini ni madhalili; na ahadi walio waahidi Waumini kuwa watawatoa mji wakisha rejea Madina. Sura imebainisha wepi katika makundi mawili hayo walio watukufu na wenye nguvu.

Na khatimaye Sura inaelekeza kuwasemeza Waumini watoe kwa ajili ya Njia ya Mwenyezi Mungu, wafanye haraka kwa hayo kabla mauti hayajamfikia mmoja wao, akajuta, na akatamani laiti inge akhirishwa ajali yake. Na wala Mwenyezi Mungu hamuakhirishi yeyote ikisha fika ajali yake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Wanapo kujia wanaafiki husema: Tunashuhudia ya kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anajua kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu anashuhudia ya kuwa hakika wanaafiki ni waongo.¹
2. Wamevifanya viapo vyao ni kinga, na wao wakajizuia kuifuata Njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika ni mabaya kabisa waliyo kuwa wakiyafanya.²
3. Hayo ni kwa sababu ya kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo umepigwa muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawafahamu lolote.³
4. Na unapo waona, miili yao inakupendeza, na wakisema, unasikiliza usemi wao. Lakini wao ni kama magogo yaliyo egemezwa. Wao hudhania kila ukelele unao pigwa ni kwa ajili yao. Hao ni maadui; tahadhari nao. Mwenyezi Mungu awaangamizilie

1 Ewe Muhammad! Wanapo kujia wanaafiki, wanasema kwa ndimi zao: Tunashuhudia kuwa hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anajua kwamba wewe ni Mtume wake; na Mwenyezi Mungu anashuhudia kwamba wanaafiki hapana shaka ni waongo katika kujidai kwao wanaamini, kwani hawasadiki katika nyoyo zao.

2 Wamezifanya yamini zao za uwongo ni kinga, au ngao za kujikingia ili wasichukuliwe kuwa ni makafiri. Basi wakajizuia wenyewe wasiishike Njia ya Mwenyezi Mungu Iliyo Nyooka. Hakika ni mabaya mno hayo wanayo yatenda ya naafiki na kujitia imani ya uwongo.

3 Hayo waliyo yafanya ndiyo mazoea ya kudhihirisha yasiyo ya kweli, na kuapa yamini za uwongo, kwa sababu hao wameamini kwa ndimi zao, kisha wakakufuru katika nyoyo zao, basi nyoyo zao zimepigwa muhuri kwa ukafiri huu. Hao hawafahamu yepi ya kuwaokoa na adhabu za Mwenyezi Mungu.

mbali! Vipi wanapotoka na haki?⁴

5. Na wanapo ambiwa: Njooi ili Mtume wa Mwenyezi Mungu akuombeeni maghfira, huvigeuza vichwa vyao, na unawaona wanageuka nao wamejaa kiburi.⁵

6. Sawa sawa kwao, ukiwatakia maghfira au hukuwatakia maghfira, Mwenyezi Mungu hatawaghufiria. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu.⁶

7. Hao ndio wanao sema: Msitoe mali kwa ajili ya walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ili waondokelee mbali! Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye khazina za mbingu na ardhi, lakini wanaafiki hawafahamu.⁷

8. Wanasema: Tukirejea Madina mwenye utukufu zaidi bila ya shaka atamfukuza aliye mnyonge. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye utukufu - Yeye, na Mtume wake, na Waumini. Lakini wanaafiki hawajui.⁸

9. Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio walio khasiri.⁹

10. Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?¹⁰

11. Wala Mwenyezi Mungu hataiakhirisha nafsi yoyote inapo fika ajali yake; na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.¹¹

4 Na ukiwaona miili yao inakupendeza kwa uzuri wao, na wakizungumza unavutika kuwasikiliza kwa utamu wa maneno yao. Kumbe wao juu ya yote hayo nyoyo zao zitupu, hazina Imani ndani yake. Kama magogo yaliyo egemezwa, hayana uhai wowote. Wao hudhania kila linalo zuka basi linawalenga wao, kwa sababu wanaitambua hali yao ya unaafiki. Hao ndio maadui, basi tahadhari nao. Mwenyezi Mungu kesho wafukuza kwenye rehema yake. Vipi wanavyo iacha Haki wakauendea unaafiki wanao ushikilia?

5 Na wakiambiwa: Jongeeni, apate Mtume wa Mwenyezi Mungu kukuombeeni msamaha, hutikisa vichwa vyao kwa kejeli, na utawaona wanageuka kwa kiburi hawataki kut'ii.

6 Ni sawa kwa hawa wanaafiki, ukiwaombea msamaha, au ukito waombea. Kwa sababu hao hawauachi unaafiki wao. Basi Mwenyezi Mungu hatawasamehe kabisa. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi kuwapeleka kwenye Haki wale wanao kataa kufuata amri yake na kumuamini.

7 Hao wanaafiki ndio wanao waambia watu wa Madina: Msitoe chochote kuwapa hao Waumini walio na Mtume wa Mwenyezi Mungu ili wapate kumwacha! Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye khazina zote za mbinguni na duniani, na riziki zote ziliomo humo. Lakini wanaafiki hawajui hayo.

8 Wanaafiki wanasema kwa kutoa ahadi: Tukirejea Madina hapana shaka kikundi chetu, ambacho ndicho chenye nguvu zaidi, kitakitoa kikundi cha Waumini ambao ni wanyonge! Nguvu anazo Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Waumini; sio hawa wanao jitia kuahidi. Lakini wanaafiki hawajui kitu.

9 Enyi mlio msadiki Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Yasikuhangaisheni mali yenu, na watoto wenu, hata mkaacha kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kutekekeleza aliyo kuamrisheni kuyafanya. Na wenye kushughulishwa na mali zao na watoto wao wakaacha hayo, basi hao ndio watao kuwa wamekhasiri Siku ya Kiyama.

10 Enyi Waumini! Toeni katika mali tuliyo kuruzukuni upesi upesi kabla mmoja wenu hayajamfikia mauti akasema kwa majuto: Ewe Mola wangu Mlezi! Hebu hunipi muhula kidogo, nikapata kutoa sadaka, na nikawa miongoni wa watu wema watendao vitendo vyema?

11 Wala Mwenyezi Mungu hampi muhula mtu yeyote ukisha fika wakati wake wa kufa. Na Mwenyezi Mungu ni Mkamilifu wa kujua yote myatendayo, na Yeye atakulipeni kwa hayo.

Sura 64 - Attaghaabun

Utangulizi

Imeanzia Sura hii kwa kueleza kuwa kila kiliomo katika mbingu na katika ardhi kinamtakasa Mwenyezi Mungu na kisio laiki na utukufu wake, na kwamba Yeye ndiye Mwenye Ufalme na Mwenye sifa njema zote, na kwamba Yeye ni Muweza wa kila kitu. Kisha hayo yakafuatilizwa na kutajwa baadhi ya dalili za utimilivu wa uweza wake na ujuzi wake. Kisha Sura ikatupa macho kuwaangalia makafiri walio kuwa kabla ya hawa, na wakawaasi Mitume wa Mola wao Mlezi, na kwamba wao walionja matokeo maovu ya vitendo vyao. Na hayo yalikuwa hivyo kwa sababu Mitume wao walipo kuwa wakiwajia kwa hoja, waliwakataa na wakawapuza! Sura tena ikaingia baada ya hayo kuvunja madai ya makafiri kwamba wao ati hawatafufuliwa. Na ikawataka watu wamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Nuru iliyo teremshwa juu yake. Na ikawahadharisha na Siku ya Mkusanyo, siku kutapo dhihiri kupunjana kwa watu. Kwani wale walio amini na wakatenda mema watapata kufuzu kukubwa, na walio kufuru ndio watakuwa watu wa Motoni, na hayo ndiyo marudio maovu. Na hakika masaibu yatakuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na hakika mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu ndio anauongoa moyo wake.

Sura inawataka watu wamt'i Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Wakipuuza, basi hakika Mtume hana juu yake ila kufikisha Ujumbe. Na inawaambia Waumini kuwa mali yao na watoto wao ni fitna, majaribio. Basi isiwe kuyashughulikia hayo kukawapelekea kuacha waliyo amrisha. Kisha ikawaamrisha wamche Mwenyezi Mungu kwa kadri wawezavyo. Na Sura ikakhitimisha kwa kuwakhushisha Waumini watoe katika njia za kheri, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushukuru, Mpole, Mjuzi wa yaliyo fichikana na yanayo onekana. Basi atawalipa kwa mali yao wanayo yatumia. Na kwamba Yeye ni Mwenye nguvu asiye shindika, Mwenye hikima, hafanyi upuuzi.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Kinamtakasa Mwenyezi Mungu kila kilichomo katika mbingu na katika ardhi. Ufalme ni wake, na sifa njema ni zake. Na Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.¹
2. Yeye ndiye aliye kuumbeni. Miongoni mwenu yupo aliye kafiri, na yupo aliye Muumini. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yatenda.²
3. Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki, na akakupeni sura, na akazifanya nzuri sura zenu. Na marudio ni kwake.³

1 Vitu vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi vinamtakasa Mwenyezi Mungu na kila kisicho kuwa laiki na utukufu wake. Yeye ndiye peke yake Mwenye ufalme ulio timia, na Mwenye sifa njema, na ndiye Mwenye uweza ulio timia juu ya kila kitu.

2 Yeye peke yake ndiye aliye kuumbeni mlipo kuwa si chochote. Basi kati yenu yupo anaye kanya Ungu wake, na miongoni mwenu yupo anaye sadiki. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yatenda, na atakulipeni kwa mujibu wa vitendo vyenu.

3 Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa hikima isiyo na ukomo, na akakuumbeni kwa

4. Anajua viliomo katika mbingu na ardhi, na anajua mnayo yaficha na mnayo yatangaza. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliomo vifuani.⁴
5. Kwani haikukujieni khabari ya walio kufuru kabla, wakaonja matokeo mabaya ya mambo yao? Na wao wana adhabu iliyo chungu.⁵
6. Hayo ni kwa kuwa walikuwa wakiwajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi, nao wakasema: Hivyo binaadamu ndio atuongoe? Basi wakakufuru, na wakageuka upande. Mwenyezi Mungu akawa hana haja nao. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, si mhitaji, naye ni Msifiwa.⁶
7. Walio kufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: Kwani? Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana shaka mtaambiwa mliyo yatenda. Na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.⁷
8. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Nuru tuliyo iteremsha. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.⁸
9. Siku atakayo kukusanyeni kwa ajili ya Siku ya Mkusanyiko; hiyo ni siku ya kupunjana. Na anaye muamini Mwenyezi Mungu na akatenda mema, atamfutia maovu yake, na atamuingiza katika Mabustani yenye kupitiwa kati yake na mito, watadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.⁹
10. Na walio kufuru na wakakadhibisha Ishara zetu, hao ni watu wa Motoni, watadumu humo milele. Na hayo ndiyo marudio mabaya.¹⁰
11. Haufiki msiba wowote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu huuongoa moyo wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.¹¹

sura, na akazifanya nzuri sura zenu, kwa kuwa amewafanya wanaadamu ndio viumbe walio nyooka vizuri. Na kwake Yeye ndiyo marejeo Siku ya Kiyama.

4 Yeye Mwenyezi Mungu anajua yote yaliomo katika mbingu na ardhi, na anayajua mnayo yaficha, na mnayo yaeneza, ikiwa maneno au vitendo. Na Mwenyezi Mungu ametimia ujuzi wake kwa mnayo dhamiria katika nyoyo zenu.

5 Zimekwisha wafikieni khabari za walio kufuru kabla yenu, na wao wakameza ubaya wa matokeo wa mambo yao katika dunia. Na Akhera watapata adhabu yenye machungu makali.

6 Masaibu hayo yaliyo wapata ni kwa sababu Mitume wao waliwajia na miujiza iliyo dhaahiri, nao wakasema kwa kukanya: Ati atujie mtu kama sisi kutuongoza? Wakakanya kuwa watafufuliwa. Wakaiacha Haki. Mwenyezi Mungu akadhihirisha kuwa hana haja na imani yao kwa kuwaangamiza. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kutimia ukwasi wake (kujitoshwa kwake), si Mwenye kuwa na haja na viumbe vyake. Ni Mwenye kustahiki kusifiwa na kuhimidiwa kwa uzuri wa neema zake.

7 Makafiri wamedai kwa uwongo kwamba hawatafufuliwa baada ya kufa kwao. Ewe Muhammad! Waambie: Mambo sio kama mnavyo dai nyinyi. Ninaapa kwa Mola wangu Mlezi! Hapana shaka yoyote nyinyi mtafufuliwa baada ya kufa kwenu, na hapana shaka yoyote kuwa mtaambiwa mliyo yatenda duniani. Kisha mtalipwa kwayo. Na huko kufufuliwa, na kuhisabiwa, na kulipwa, ni jambo sahali na jepesi kabisa kwa Mwenyezi Mungu.

8 Basi msadikini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na ongokei kwa kuifuata Nuru tuliyo mteremshia hata akakufahamisheni kwa uwazi kuwa kufufuliwa kunakuja bila ya shaka yoyote. Na Mwenyezi Mungu ana ujuzi wa kutumia kwa yote yanayo tokana nanyi.

9 Siku atapo kukusanyeni katika Siku ya Mkusanyo wa walio tangulia mwanzo na walio kuja mwisho, akulipeni kwa vitendo vyenu! Siku hiyo ndiyo Siku ya Taghaabun, Kupunjana, kutapo dhiri kupunjika kwa makafiri kwa kuacha Imani, na kupunjika Waumini kwa kupuuzia kuongeza ut'iifu. Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na akatenda mema atamwondolea maovu yake, na atamtia katika Bustani zenye kupita kati yake mito, wakae humo milele. Malipo hayo ndio kufuzu kukubwa.

10 Na walio ikataa Imani, na wakaikanusha miujiza yetu tuliyo wapa Mitume wetu kuwanga mkono, hao ndio watu wa Motoni. Watadumu humo. Na marudio maovu ni hayo walio yarudia hao.

11 Mja hasibiwi na balaa ila kwa kudra ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumsadiki Mwenyezi Mungu

12. Na mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume. Mkigeuka, basi hakika juu ya Mtume wetu ni kufikisha (Ujumbe wake) kwa uwazi tu.¹²
13. Mwenyezi Mungu, hapana mungu isipo kuwa Yeye. Na juu ya Mwenyezi Mungu nawategemee Waumini.¹³
14. Enyi mlio amini! Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu. Basi tahadharini nao. Na mkisamehe, na mkapuuzza, na mkaghufiria basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, Mwenye kurehemu.¹⁴
15. Hakika mali yenu na watoto wenu ni jaribio. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa.¹⁵
16. Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo, na sikieni, na t'iini, na toeni, itakuwa kheri kwa nafsi zenu. Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio walio fanikiwa.¹⁶
17. Mkimkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri, atakuzidishieni mardufu, na atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa shukra, Mpole.¹⁷
18. Mwenye kujua siri na dhaahiri, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.¹⁸

basi humwongoa moyo wake kwendea katika yanayo mpendeza. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kutimia ujuzi wake.

12 Na mt'iini Mwenyezi Mungu kwa aliyo kuamrisheni, na mt'iini Mtume kwa Ujumbe aliyo kufikishieni kutoka kwa Mola wake Mlezi. Mkiupuuzza ut'iifu huu, basi Yeye hadhuriki kitu kwa mapuuzza yenu. Na hakika Mtume wetu hana jukumu juu yake ila kufikisha Utume wake tu kwa uwazi.

13 Mwenyezi Mungu, hapana wa kuabudiwa kwa haki isipo kuwa Yeye tu peke yake. Basi Waumini nawamtegemee Yeye tu katika mambo yao yote.

14 Enyi mlio amini! Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu, ambao wanakuzuilieni msimt'ii Mwenyezi Mungu kwa kutaka kuwatimizia hao matakwa yao. Basi kuweni na hadhari nao. Na mkiweza kuyavuka makosa yao yanayo kubalika kusameheka, na mkayapuuzza, na mkawafichia, basi Mwenyezi Mungu naye atakughufirieni nyinyi. Kwani hakika Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu wa maghfira na rehema.

15 Hakika mali yenu na watoto wenu ni majaribio na mtihani. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa kwa anaye pendelea kumt'ii Mwenyezi Mungu..

16 Basi tumieni juhudi zenu na nguvu zenu katika kumcha Mwenyezi Mungu. Na sikieni mawaidha yake, na t'iini amri zake, na toeni katika alichokuruzukuni kwa ajili ya hicho alichokurusha kitolewe kwa ajili yake. Na tendeni kheri kwa sababu ya nafsi zenu. Na mwenye kuzuiliwa na Mwenyezi Mungu ubakhili na uchoyo wa roho yake, basi watu kama hao ndio walio jaaliwa kupata kila kheri.

17 Mkitoa katika mambo ya kheri kutoa kwa moyo safi, basi Mwenyezi Mungu atazidisha mardufu thawabu za mlichotoa, na atakusameheni madhambi yenu yaliyo kuponyokeni. Na Mwenyezi Mungu ni Mkuu wa shukrani, na kuwalipa watendao mema, na ni Mpole, hafanyi haraka kuwaadhibu wanao muasi.

18 Yeye ni Mjuzi wa vilivyo fichikana na vinavyo onekana, Mwenye nguvu, Mtenda nguvu, Mwenye hikima katika mipango ya viumbe vyake, Mwenye kuweka kila kitu kwa pahala pake.

Sura 65 - Att'alaq

Utangulizi

Sura hii inaeleza baadhi ya hukumu za talaka, na eda, na namna zake, na hukumu zake - tangu kubaki mwenye eda katika nyumba aliyo pewa talaka ndani yake, na waajibu wa kumtazama kwa matumizi, na maskani. Na kati ya hukumu hizi, kama ilivyo mwendo wa Qur'ani, ipo ahadi kwa mwenye kufuata amri za Mwenyezi Mungu, na onyo kwa mwenye kukiuka mipaka yake. Kisha Sura imeashiria malipo ya wenye kutakabari wakakataa kutimiza amri za Mwenyezi Mungu na Watume wake. Na ikakhitimisha Sura kwa kuwahimiza Waumini wamche Mwenyezi Mungu, na kuwakumbusha neema za kuwapelekea Mtume anaye wasomea Aya za Mwenyezi Mungu, ili awatoe kwenye giza wende kwenye mwangaza, na kwa uweza wake Mwenyezi Mungu kuziumba mbingu saba, na katika ardhi mfano wa hizo.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ewe Nabii! Mtakapo wapa talaka wanawake, basi wapeni talaka katika wakati wa eda zao. Na fanyeni hisabu ya eda. Na mcheni Mwenyezi Mungu, Mola wenu Mlezi. Msiwatoe katika nyumba zao, wala wasitoke wenyewe, ila wakifanya jambo la uchafu ulio wazi. Hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu, msiikiuke. Na mwenye kuikiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi amejidhulumu nafsi yake. Hujui; labda Mwenyezi Mungu ataleta jambo jengine baada ya haya.¹

2. Basi wanapo fikia muda wao, ima warejeeni muwaweke kwa wema, au farikianeni nao kwa wema. Na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu. Na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo anavyo agizwa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na anaye mcha Mwenyezi Mungu humtengezea njia ya kutokea.²

3. Na humruzuku kwa jiha asiyo tazamia. Na anaye mtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake.³

1 Ewe Nabii! Mkitaka kuwapa talaka wanawake, basi wapeni talaka kwa kukabiliana na eda zao, (yaani wakati wa tahara kabla ya kuwaingilia), na idhibitini eda, na mcheni Mwenyezi Mungu, Mola wenu Mlezi. Msiwatoe watalaka katika nyumba zao walimo pewa talaka. Wasitoke humo ila ikiwa wamefanya kitendo kichafu wazi. Hukumu hizo zilizo tangulia ni alama za Mwenyezi Mungu amezifanya ni sharia kwa waja wake. Na Mwenye kukiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu basi amejidhulumu nafsi yake. Hujui pengine Mwenyezi Mungu labda ataleta jambo usilo litaraji baada ya talaka hiyo, na wakapendana.

2 Wakikaribia walio achwa mwisho wa eda zao warejeeni mkae nao kwa wema na ihsani, au farikianeni nao bila ya madhara. Na washuhudishe kuwarejea na kufarikiana watu wawili waadilifu miongoni mwenu, na toeni ushahidi kwa mujibu wake kwa kumsafia Mwenyezi Mungu. Hayo mliyo amrisha ndiyo anayo waidhiwa mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na mwenye kumkhofu Mwenyezi Mungu akazishika amri zake na akaepuka makatazo yake atamjaalia njia ya kutokana na kila dhiki.

3 Na atamtengezea sababu za kupata riziki kwa jiha ambazo hata hazimpitiki katika fikra zake. Na mwenye kumwachia mambo yake yote Mwenyezi Mungu basi Yeye ni Mwenye kumtosha, hana haja ya mwengine. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kutimiza alitakalo, ni Mwenye kutekeleza alipendalo. Amejaalia kila kitu na wakati wake, wala haupitikii, na kipimo hakivuki.

4. Na wale walio sita hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, pamoja na ambao hawapati hedhi. Na wenye mimba eda yao mpaka watakapo zaa. Na anaye mcha Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu humfanyia mambo yake kuwa mepesi.⁴
5. Hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu amekuteremshieni. Na anaye mcha Mwenyezi Mungu atamfutia maovu yake, na atampa ujira mkubwa.⁵
6. Wawekeni humo humo mnamo kaa nyinyi kwa kadiri ya pato lenu, wala msiwalettee madhara kwa kuwadhiki. Na wakiwa wana mimba, wagharimieni mpaka wajifungue. Na wakikunyonyesheeni, basi wapeni ujira wao, na shaurianeni kwa wema. Na mkiona uzito kati yenu, basi amnyonyeshee mwanamke mwengine.⁶
7. Mwenye wasaa atoe kadiri ya wasaa wake, na mwenye dhiki atoe katika alichu mpa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hamkalifishi mtu ila kwa kadiri ya alichu mpa. Mwenyezi Mungu atajaalia baada ya dhiki faraji.⁷
8. Na miji mingapi iliyo vunja amri ya Mola wake Mlezi na Mitume wake, basi tuliihisabia hisabu ngumu na tukaiadhibu kwa adhabu kali.⁸
9. Basi ikauonja ubaya wa mambo yake; na mwisho wa mambo yao ilikuwa khasara.⁹
10. Mwenyezi Mungu aliwaandalia adhabu kali. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili, mlilo amini! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteremshieni Ukumbusho,¹⁰
11. Mtume anaye kusomeeni Aya za Mwenyezi Mungu zinazo bainisha, ili kuwatoa walio amini na wakatenda mema kutoka gizani kuwapeleka kwenye nuru. Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na akatenda mema, atamwingiza katika Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Mwenyezi Mungu amekwisha mpa

4 Na wenye eda ya talaka miongoni mwa wanawake walio sita kuingia myezini kwa utu uzima, kama hawajui wahisabu vipi eda yao, basi eda yao ni miezi mitatu. Na wale ambao hawaingii hedhi kabisa ni kadhaalika. Na wenye mimba, eda yao inakwisha wanapo jifungua. Na mwenye kumcha Mwenyezi Mungu, na akazitimiza hukumu zake Mwenyezi Mungu atamsahilishia mambo yake.

5 Sharia hizo ni amri ya Mwenyezi Mungu, si ya mwengine. Amekuteremshieni Yeye. Na mwenye kumcha Mwenyezi Mungu kwa kuzihifadhi hukumu zake humfutia makosa yake, na akayafanya makubwa malipo yake.

6 Wawekeni wanawake waliomo edani humo humo katika nyumba zenu, kwa kadiri ya uwezo wenu. Wala msiwalettee madhara yoyote, kuwaletea dhiki katika maskani. Na ikiwa wana mimba basi watoleeni gharama za kuwakimu mpaka wazaa. Wakikunyonyesheeni watoto wenu hao watalaka, basi wapeni ujira wao. Na amrیشانeni mambo mazuri ya kusameheana na kuacha kutaabishana. Na ikitokea kati yenu dhiki na taabu, basi baba atafute mnyonyeshaji mwengine badala ya mama aliye achwa.

7 Atoe mwenye nafasi nzuri ya riziki kwa mujibu alichu kunjuliwa na Mwenyezi Mungu, na mwenye dhiki ya pato atoe kwa kadiri alichu mpa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hamkalifishi mtu ila kwa mujibu alichu mpa. Mwenyezi Mungu atajaalia baada ya dhiki faraji.

8 Na miji mingi ambayo watu wake wamefanya ujabari na wkapuuza amri ya Mola wao Mlezi na Mitume wake, tukaihisabia kwa hisabu kali kwa kuchungua kila walilo litenda na kujadiliana nao, na tukawaadhibu adhabu ya kuchusha iliyo mbaya, wakagugumia malipo maovu ya mambo yao. Na ukawa mwisho wa mambo yao ni kukhasiri kukubwa mno.

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Mwenyezi Mungu amewaandalia watu wa miji ya watu walio fanya ujabari adhabu ya mwisho wa ukali. Basi tahadharini na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili sawa, ambao mnasifika kwa Imani. Amekuteremshieni mtu mwenye utukufu na cheo, Mtume anaye kusomeeni Aya za Mwenyezi Mungu zenye kukubainishieni baina yaliyo kweli na ya uwongo, ili awatoe walio amini na wakatenda mema kutoka kwenye giza la upotovu kwenda kwenye mwangaza wa hidaya. Na mwenye kumsadiki Mwenyezi Mungu, na akatenda vitendo vyema atamtia katika Bustani zinazo pita kati yake mito. Watakaa humo milele. Mwenyezi Mungu kamfanyia ihsani Muumini mwema kwa kumpa riziki iliyo njema.

riziki nzuri.¹¹

12. Mwenyezi Mungu ni yule ambaye ameziumba mbingu saba, na ardhi kwa mfano wa hizo. Amri zake zinashuka baina yao, ili mjue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu, na kwamba Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu kukijua vilivyo kwa ilimu yake.¹²

¹¹ Tazama tanbihi ya 10.

¹² Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye umbaa mbingu saba, na ardhi mfano wa hizo. Amri yake inapita kote, ili mjue kwamba Mwenyezi Mungu ni mtimilivu wa uweza, na kwamba Mwenyezi Mungu amevizunguka vitu vyote kwa ujuzi wake.

Sura 66 - Attah'riim

Utangulizi

Sura hii inaashiria jambo ambalo lilimuudhi Nabii s.a.w. katika baadhi ya wake zake; akajizuilia na baadhi ya mambo ambayo nafsi huyapenda na Mwenyezi Mungu amehalalisha. Na inawahadharisha wake zake na matokeo ya waliyo yatenda. Kisha Sura ikaingia kuwaamrisha Waumini wajikinge nafsi zao na ahali zao na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Na ikabainisha kwamba haukubalii udhuru wa makafiri Siku ya Kiyama. Na inawataka Waumini watubu kweli kweli, na Mtume s.a.w. ende kupambana kwa Jihadi na makafiri na wanaafiki, na awe mgumu kwao. Na inakhitimisha kwa kupiga mifano kwamba wema wa waume hautazuia adhabu isiwapikie wake zao wakiwa wao wamepotoka, na kwamba uharibifu wa waume hauwadhuru wake zao ikiwa hao wake wamesimama sawa sawa. Kwani kila nafsi ina dhamana kwa vitendo vyake mwenyewe.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ewe Nabii! Kwa nini unaharimisha alichokuhalilishia Mwenyezi Mungu? Unatafuta kuwaridhi wake zako. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.¹
2. Hakika Mwenyezi Mungu kakupeni Sharia ya kufungua viapo vyenu, na Mwenyezi Mungu ni Mola wenu. Na Yeye ni Mwenye kujua, Mwenye hikima.²
3. Na Nabii alipo mwambia mmoja wa wake zake jambo la siri. Basi alipo litangaza yule mke, na Mwenyezi Mungu akamdhihirishia Mtume, alimjuvya sehemu na akaacha sehemu nyengine. Alipo mwambia hayo, huyo mke akasema: Nani aliye kwambia haya? Mtume akasema: Kaniambia Mjuzi Mwenye khabari zote!³
4. Kama nyinyi wawili hamkutubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyo zenu zimekwisha elekea huko. Na mkisaidiana dhidi yake (Mtume), basi hakika Mwenyezi Mungu ndiye kipenzi chake, na Jibrili, na Waumini wema, na zaidi ya hayo Malaika pia watasaidia.⁴

1 Ewe Nabii! Kwa nini unajikhini nafsi yako alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu? Unataka kuwaridhi wakezo, na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mkunjufu wa kurehemu.

2 Amekuwekeeni Sharia ya kuondoa viapo vyenu kwa kafara. Na Mwenyezi Mungu ni Bwana wenu, Mwenye kutawala mambo yenu, na Yeye ni Mtamilivu wa ujuzi, basi anakuwekeeni Sharia zenye kheri yenu, naye ni Mwenye hikima katika kuweka Sharia zake.

3 Na taja pale Nabii alipo msimulia jambo kwa siri mmoja katika wake zake, na alipo ifichua. Na Mwenyezi Mungu akamjuvya Nabii wake kuwa imefichuliwa. Akamjuvya baadhi, na akamzuilia - kwa staha - baadhi nyengine. Alipo mjuvya, akasema yule mke: Nani aliye kwambia haya? Akasema Nabii: Ameniambia Mwenye kujua kila kitu, asiye fichika kitu.

4 Mkirejewa nyinyi wawili kwa Mwenyezi Mungu nanyi mmejuta basi itakuwa mmefanya waajibu wenu wa kutubu, kwa sababu nyoyo zenu zilikuwa zimeacha jambo analo lipenda Mtume wa Mwenyezi Mungu, nalo ni kuweka siri. Na ikiwa mtasaidiana kinyume chake kwa mambo ya kumuudhi, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Msaidizi wake, na Jibrili, na Waumini wanao sifika kwa wema, na Malaika baada ya msaada wa Mwenyezi Mungu nao ni wenye kumsaidia.

5. Asaa Mola wake Mlezi, akikupeni talaka, akampa wake wengine badala yenu nyinyi, walio bora kuliko nyinyi, wanyenyekevu, Waumini, wat'awa, walio tubu, wenye kushika ibada, wafanyao kheri, wajane na wanawari.⁵
6. Enyi mlio amini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrishwa.⁶
7. Enyi mlio kufuru! Msilete udhuru leo. Hakika mnalipwa mliyo kuwa mkiyatenda.⁷
8. Enyi mlio amini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli! Asaa Mola wenu Mlezi akakufutieni maovu yenu na akakuingizeni katika Pepo zipitazo mito kati yake, siku ambayo Mwenyezi Mungu hatamdhalilisha Nabii na walio amini pamoja naye. Nuru yao inakwenda mbele yao na pande zao za kulia, na huku wanasema: Mola wetu Mlezi! Tutimilizie nuru yetu, na utughufirie! Hakika Wewe ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.⁸
9. Ewe Nabii! Pambana na makafiri na wanaafiki, na kuwa mgumu kwao! Na makaazi yao ni Jahannamu. Na hayo ni marejeo mabaya.⁹
10. Mwenyezi Mungu amewapigia mfano walio kufuru: mke wa Nuhu na mke wa Lut'i. Walikuwa chini ya waja wetu wema wawili miongoni mwa waja wetu. Lakini wakawakhuni waume zao, nao wasiwafae kitu. Na ikasemwa: Ingieni Motoni pamoja na wanao ingia!¹⁰
11. Na Mwenyezi Mungu amewapigia mfano walio amini - mkewe Firauni, alipo sema: Mola wangu Mlezi! Nijengee kwako nyumba Peponi, na uniokoe na Firauni na vitendo vyake, na uniokoe na watu madhaalimu.¹¹

5 Asaa Mola wake Mlezi akikuacheni, enyi wakeze, atamwoza badala yenu wake wengine walio wanyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu kwa ut'iifu, wenye kusadiki kwa nyoyo zao, wanyonge mbele ya Mwenyezi Mungu, wenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu kwa toba, wenye kumuabudu kwa kujidhalilisha kwake, wendao kila njia za ut'iifu kwa Mwenyezi Mungu, wajane na bikra.

6 Enyi mlio amini! Jihifadhini nafsi zenu na ahali zenu na Moto, ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanao simamia kazi yake na kuwaadhibu waliomo humo ni Malaika wakali, na wana nguvu katika muamala wao. Na wao hutekeleza lile wanalo amrishwa, wala hawakawilishi.

7 Wataambiwa makafiri Siku ya Kiyama: Msitafute udhuru leo! Hapana shaka mnalipwa mliyo kuwa mkiyatenda.

8 Enyi mlio amini! Rejeeni kwa Mwenyezi Mungu, muache madhambi yenu, mrejee kweli kweli kwa ikhlasi. Asaa Mola wenu Mlezi akakufutieni maovu yenu, na akakutieni Peponi kwenye kupita mito chini ya majumba yake na miti yake, Siku atakayo inyanyua Mwenyezi Mungu hadhi ya Nabii na walio amini pamoja naye. Nuru yao hao itakuwa inakwenda mbele yao, nayo itakuwa kuliani mwao, nao watakuwa wakisema kwa kujikaribisha kwa Mwenyezi Mungu: Ewe Bwana wetu, Mwenye kumiliki mambo yetu! Tutimizie nuru yetu, mpaka tuongoke kufikia Peponi. Na tusamehe dhambi zetu. Hakika Wewe ni Mtamilivu wa uweza juu ya kila kitu.

9 Ewe Nabii! Pambana kwa Jihadi na hao walio tangaza ukafiri wao, na wanaafiki walio uficha ukafiri wao, kwa kila unacho kimiliki, nguvu na hoja. Na kuwa mkali juu ya makundi yote mawili hayo katika Jihadi yako. Na makaazi ya hao ni Jahannamu. Na marejeo maovu ni hayo marejeo yao!

10 Mwenyezi Mungu ametaja hali ya ajabu inayo juulikana kuwa ni hali zinazo fanana kwa wanao kufuru. Nayo ni hali ya mke wa Nuhu na mke wa Lut'i. Hao walikuwa chini ya ulinzi wa waja wawili katika waja wema. Nao wakawakhuni kwa kupanga njama dhidi yao, na kufichua siri zao kwenda wambia kaumu zao. Na waja wema wawili hawakuweza kuwakinga wake zao kwa lolote katika adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na wakaambiwa hao wake wawili walipo angamizwa: Ingieni Motoni pamoja na wanao ingia.

11 Na Mwenyezi Mungu amepiga mfano kwa Waumini kisa cha mke wa Firauni alipo sema: Mola wangu Mlezi! Nijengee kwako nyumba karibu na rehema yako Peponi, na uniokoe na utawala wa Firauni na vitendo vyake vilivyo pita mipaka katika dhulma, na uniokoe na kaumu ya wanao fanya uadui!

12. Na Mariamu binti wa Imrani, aliye linda ubikira wake, na tukampulizia humo kutoka roho yetu, na akayasadiki maneno ya Mola wake Mlezi na Vitabu vyake, na alikuwa miongoni mwa wat'iifu.¹²

12 Na Mwenyezi Mungu amewapigia Waumini mfano wa Mariamu binti wa Imrani, ambaye amehifadhi utupu wake, tukampulizia humo katika roho yetu, akashika mimba ya Isa. Naye akayasadiki maneno ya Mwenyezi Mungu, nayo ni amri zake, na makatazo yake, na Vitabu vilivyo teremshwa juu ya Mitume wake. Na yeye alikuwa miongoni mwa idadi walio dumu juu ya ut'iifu wa Mwenyezi Mungu. (Huku kupuliziwa Mariamu roho ya Mwenyezi Mungu si kiroja, kwani wanaadamu wote wamepuliziwa kadhaalika. Soma Surat Al-H'ijr Aya 28-29 inapo simuliwa alipo umbwa mtu na akapuliziwa kutokana na roho ya Mwenyezi Mungu.)

Sura 67 - Al-Mulk

Utangulizi

Sura hii inaitwa Surat Al-Mulk kwa kutokana na neno *Al-Mulk*, yaani Ufalme, linalo tokea katika Aya ya kwanza katika Sura. Na muhimu ya makusudio ya Sura hii tukufu ni kuelekeza fikra na nadhari zizingatie athari ya uweza wa Mwenyezi Mungu ulio zagaa katika nafsi za watu na katika viumbe vya Mwenyezi Mungu mnavyo viona katika ardhi na mbinguni upeo wa macho yenu, ili hayo yawe ndiyo njia ya kupelekea kumuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na pia Sura hii inabainisha hali ya makafiri ambao watatupwa katika Jahannamu, na watasikilizana mikoromo yao, na wataungua katika Moto wake, na wataungama madhambi yao, na watajuta kwa watavyo ishia, watapo wauliza Malaika kwa kuto mwitikia Mtume alipo waita na akawahadharisha.

Na ama walio mkhofu Mola wao Mlezi, na wakamuamini, hao watapata maghfira na msamaha kwa makosa yaliyo waporonyoka, na ujira mkubwa kwa mema waliyo yatanguliza na wakayatenda.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. AMETUKUKA ambaye mkononi mwake umo Ufalme wote; na Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.¹
2. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha.²
3. Aliye umba mbingu saba kwa matabaka. Huoni tafauti yoyote katika uumbaji wa Mwingi wa Rehema. Hebu rudisha nadhari! Unaona kosa lolote?³
4. Tena rudisha nadhari mara mbili, nadhari yako itakurejea mwenyewe hali ya kuwa imehizika nayo imechoka.⁴
5. Na kwa hakika tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa, na tumeyafanya ili kuwapigia mashetani, na tumewaandalia adhabu ya Moto uwakao kwa nguvu.⁵
6. Na kwa walio mkufuru Mola wao Mlezi ipo adhabu ya Jahannamu. Na ni marejeo

1 Ametukuka, na amezidi baraka zake Mwenye kumiliki peke yake uwezo wa kuendesha mambo ya viumbe vyote. Na Yeye, juu ya kila kitu, anao uwezo ulio timia.

2 Ambaye ndiye aliye umba mauti na uhai kwa makusudio anayo yataka Yeye, ili akufanyieni mtihani ni yupi katika nyinyi anaye fanya vitendo sawa, na mwenye niya safi. Na Yeye ni Mwenye kushinda, wala hashindiki kwa kitu, Mwenye msamaha kwa wenye upungufu.

3 Yeye ndiye aliye zizua mbingu saba zilizo pandana kwa mpango mmoja sawa sawa. Huoni tafauti yoyote katika uundaji wa Mwenyezi Mungu, ambaye rehema yake imeenea kwenye viumbe vyake vyote. Basi hebu tazama tena, unaona khitilafu yoyote.

4 Kisha tazama tena, na tena! Jicho lako linakurejea mwenyewe bila ya kugundua aibu yoyote, nalo limechoka.

5 Na hakika Sisi tumeipamba mbingu hii ya karibu, unayo iona kwa macho, tumeipamba kwa nyota zinazo ng'aa. Na tumefanya katika hizo vimondo vya kuwapopolea mashetani; na Akhera tumewaandalia adhabu ya moto unao waka. (*Tazama Maelezo 67:5*)

maovu yalioje hayo!⁶

7. Watakapo tupwa humo watausikia mngurumo wake na huku inafoka.⁷

8. Inakaribia kupasuka kwa hasira. Kila mara likitupwa kundi humo walinzi wake huwauliza: Kwani hakukujieni mwonyaji?⁸

9. Watasema: Kwani! Ametujia mwonyaji, lakini tulimkadhibisha, na tukasema: Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote. Nyinyi hamumo ila katika upotovu mkubwa!⁹

10. Na watasema: Lau kuwa tungeli sikia, au tungeli kuwa na akili, tusingeli kuwa katika watu wa Motoni!¹⁰

11. Wakakiri dhambi zao. Basi kuangamia ni kwa watu wa Motoni!¹¹

12. Hakika wanao mwogopa Mola wao Mlezi kwa ghaibu, watapata maghfira na ujira mkubwa.¹²

13. Na ficheni kauli zenu, au zitangazeni; hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.¹³

14. Asijue aliye umbra, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?¹⁴

15. Yeye ndiye aliye idhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake. Na kwake Yeye ndio kufufuliwa.¹⁵

16. Mnadhani mko salama kwa alioko juu kuwa hataku didimizeni kwenye ardhi, na tahamaki hiyo inatikisika!¹⁶

17. Au mnadhani mko salama kwa alioko juu ya kuwa Yeye hakupelekeeni kimbunga chenye changarawe? Mtajua vipi maonyo yangu?¹⁷

18. Na bila ya shaka walikwisha kanusha walio kuwa kabla yao; basi kulikuwaje kukasirika kwangu?¹⁸

6 Na kwa ajili ya wasio muamini Mola wao Mlezi tumewawekea adhabu ya Jahannamu. Na huo ndio mwisho muovu kweli kwao.

7 Wakitiwa humo watasikia sauti mbaya ya kuchusha, na huo moto unatokota kwa ukali, unakaribia kukatika na kutawanyika kwa wingi wa kuwaghadhibikia. Kila likitumbukizwa kundi mojawo kati yao walinzi wake huwauliza kwa kuwajejeli: Kwani hakukujieni Mtume kukuhadharisheni na mkutano wa siku hii ya leo?

8 Tazama tanbihi 7.

9 Na wao watajibu: Ametujia mwonyaji, lakini sisi tulimkanusha tukamwambia mwongo, na tukasema: Mwenyezi Mungu hakuteremshia chochote wewe wala Mitume wengine. Nyinyi mnao dai Utume si chochote ila ni watu walio potoka, na mko mbali na haki.

10 Na watasema: Lau kuwa tulikuwa tunasikia kama inavyo faa asikie mwenye kutaka ukweli wa mambo, au tunafikiri tunayo itiwa, tusinge kuwa miongoni mwa watu wa Motoni.

11 Basi wataungama kukadhibisha kwao na kukufuru kwao. Watu wa Motoni wamepotelea mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu!

12 Hakika wenye kumkhofu Mola wao Mlezi, na hali wao hawamwoni, watafutwiwa madhambi yao, na watapata thawabu kubwa kwa mema yao.

13 Na ficheni kauli yenu, au itangazeni. Yote mawili kwa Mwenyezi Mungu ni sawa, kwani Yeye ni Mkuu wa kuyazunguka yote kwa kuyajua, Mjuzi wa vinavyo ficha vifua.

14 Kwani Muumba si Mwenye kujua mambo yote ya waja wake? Na Yeye ni Mjuzi wa dogo na kubwa.

15 Yeye ndiye aliye ifanya ardhi dhalili inakut'iini. Basi tembeeni pande zake kote kote. Na kuleni katika riziki zake zinazo toka ndani yake. Na kwake Yeye peke yake ndio kufufuliwa na kulipwa.

16 Je! Mmejiaminisha na Mwenye Ufalme wa mbinguni, kuwa hataku katieni ardhi, akakuchukuliwa kwa ghafla kwa mtikiso mkubwa?

17 Bali, mmejiaminisha na Mwenye Ufalme wa mbinguni, kuwa hatakupelekeeni upepo wa kukupopoeni kwa changarawe? Hapo basi mtakijiua kitisho cha onyo langu kwenu!

18 Na hakika walikwisha wakanusha Mitume wao hao walio kuwa kabla ya kaumu yako. Basi ghadhabu yangu juu yao ilikuwa hali gani kwa nilivyo waangamiza na kuwashika.

19. Kwani hawawaoni ndege walioko juu yao namna wanavyo zikunjua mbawa zao, na kuzikunja? Hawawashikilii ila Mwingi wa rehema. Hakika Yeye ni Mwenye kuona kila kitu.¹⁹
20. Au ni lipi hilo jeshi lenu la kukunusuruni badala ya Mwingi wa Rehema? Hakika makafiri hawamo ila katika udanganyifu.²⁰
21. Au ni nani huyo ambaye atakupeni riziki kama Yeye akizuia riziki yake? Bali wao wanakakamia tu katika jeuri na chuki.²¹
22. Je! Anaye kwenda akisinukia juu ya uso wake ni mwongofu zaidi, au yule anaye kwenda sawasawa katika Njia Iliyo Nyooka?²²
23. Sema: Yeye ndiye aliye kuumbeni tangu mwanzo, na akakupeni masikio na macho, na nyoyo. Ni kidogo kabisa shukrani zenu.²³
24. Sema: Yeye ndiye aliye kutawanyeni katika ardhi, na kwake mtakusanywa.²⁴
25. Na wanasema: Lini ahadi hii, ikiwa mnasema kweli?²⁵
26. Sema: Hakika ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu; na hakika mimi ni mwonyaji tu mwenye kubainisha.²⁶
27. Lakini watakapo iona karibu, nyuso za walio kufuru zitahuzunishwa, na itasemwa: Hayo ndiyo mliyo kuwa mkiyaomba.²⁷
28. Sema: Mwaonaje, ikiwa Mwenyezi Mungu atanihiliki mimi na walio pamoja nami, au akiturehemu, ni nani atakaye walinda makafiri na adhabu chungu?²⁸
29. Sema: Yeye ndiye Mwingi wa Rehema; tunamuamini Yeye, na juu yake tunategemea. Mtakuja jua ni nani aliye katika upotovu ulio dhaahiri.²⁹

19 Wameingia upofu? Wala hawakuwaangalia ndege walio juu yao, vipi wanavyo kunjua mbawa zao mara kwa mara, na mara nyingine wakizikunja? Hapana anaye washikilia wasianguke ila Mwingi wa Rehema. Hakika Yeye ni Mwingi wa ujuzi na khabari kwa kila kitu. Anakipa kila kitu jambo kwa mujibu wa maslaha yake. (*Tazama Maelezo 67:19*)

20 Bali ni nani huyo mwenye nguvu kwenu atakaye kulindeni na adhabu asiye kuwa Mwenyewe *Arrahman*, Mwingi wa Rehema? Makafiri hawamo ila katika udanganyifu tu kwa hayo wanayo yadhania.

21 Bali ni nani huyo atakaye kuruzukuni kwa yanayo kupeni uhai wenu na starehe zenu, ikiwa Mwenyezi Mungu akizuia riziki zake asikupeni? Bali makafiri wamekakamia katika kutakabari kwao na kuikimbia Haki.

22 Je! Hali itageuka? Mwenye kwenda akijikwaa na kusinukia juu ya uso wake ni mwongofu zaidi katika mwendo wake, au yule anaye tembea sawasawa kwenye njia isiyo kwenda upogo?

23 Sema: Huyo aliye kuumbeni nanyi hamjakuwa chochote, na akakupeni usikizi na kuona, na fahamu ambazo ni sababu za vitendo vyenu na uwongofu wenu - ama ni kuchache mno kushukuru kwenu kwa neema hizi kumshukuru huyo aliye kupeni.

24 Sema: Huyo ndiye aliye kutawanyeni katika ardhi, na kwake Yeye peke yake ndio mtarejea kwa ajili ya kukuhisabuni na kukulipeni.

25 Na wanasema wanao kanya kufufuliwa: Yatatokea lini haya ya kukusanywa watu? Twambieni yatakuwa lini, kama nyinyi mnasema kweli!

26 Ewe Muhammad! Sema: Ujuzi wa hayo ni wa Mwenyezi Mungu peke yake. Ama mimi ni mwonyaji miongoni mwa waonyaji tu.

27 Watakapo yaona hayo yaliyo ahidiwa yapo karibu nao, nyuso za makafiri zitajaa huzuni na unyonge, na wataambiwa kwa kuwakejeli na kuwatia uchungu: Haya ndiyo mliyo kuwa mkiyataka yaje kwa haraka!

28 Sema: Nambieni, ikiwa Mwenyezi Mungu akinifisha mimi na Waumini walio pamoja nami, kama mnavyo tamani yawe, au akaturehemu akaakhirisha ajali yetu, na akatusamehe asituadhibu, maana itakuwa katuokoa katika hali zote mbili, basi nani atakaye wakinga makafiri na adhabu chungu wanayo istahiki kuipata kwa sababu ya ukafiri wao, na kudanganyika kwao na miungu yao?

29 Yeye huyo ndiye *Arrahman*, Mwingi wa Rehema, tunaye msadiki sisi, na nyinyi hamumsadiki. Yeye tu peke yake ndiye tunaye mtegemea, na nyinyi mnawategemea wengine. Mtakuja jua itakapo teremka

30. Sema: Mwaonaje, yakiwa maji yenu yamedidimia chini, nani atakueleteeni maji yanayo miminika?³⁰

adhabu ni kundi gani kati yetu lilio tengeka mbali na Haki.

30 Sema: Hebu nipeni khabari, maji yenu yakitoweka chini ya ardhi msiweze kuyapata kwa namna yoyote, ni nani asiye kuwa Mwenyezi Mungu atakaye kuleteeni maji ya dhaahiri yanayo miminika anayo weza kuyapata kila atakaye?

Sura 68 - Al-Qalam

Utangulizi

Sura hii tukufu imekusanya kumtetea Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. na kuipelekea hima yake na azma yake hata abakie mwenye kushikilia Haki bila ya kumlegezea yeyote, na kushabihisha adhabu iliyo wapata watu wa Makka na adhabu iliyo wapata watu wenye shamba ambao kisa chao kimesimuliwa katika Sura. Na Waumini wanabashiriwa watayo yapata kutoka kwa Mola wao Mlezi; na hapana usawa baina yao na makafiri. Wanao kadhibisha wanakanywa madai yao wanao jidaia nafsi zao bila ya haki, na wanatiwa khofu kwa kuelezwa hali yao itakavyo kuwa Akhera, na wanatishwa. Na Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. ananasihiwa asubiri na astahamili. Mwisho Sura inakhitimisha kwa kuitukuza Qur'ani tukufu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Nuun. Naapa kwa kalamu na yale wayaandikayo,¹
2. Kwa neema ya Mola wako Mlezi wewe si mwendawazimu.²
3. Na kwa hakika wewe una malipo yasiyo katika.³
4. Na hakika wewe una tabia tukufu.⁴
5. Karibu utaona, na wao wataona,⁵
6. Ni nani kati yenu aliye pandwa na wazimu.⁶
7. Hakika Mola wako Mlezi ndiye Yeye ajuaye zaidi nani aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoka.⁷
8. Basi usiwa ii wanao kadhibisha.⁸
9. Wanatamani lau unge lainisha ili nao wakulainishie.⁹
10. Wala usimt'ii kila mwingi wa kuapa wa kudharauliwa,¹⁰

1 Nuun, ndio harufi ya N, iliyo anzia Sura hii ni kama kupinzana na hao wanao kadhibisha, na ili kuwazindua wenye kusadiki.

2 Naapa kwa kalamu wanayo andikia Malaika na wenginewe, na hayo mambo ya kheri na manufaa wanayo yaandika, hakika wewe, na Mwenyezi Mungu amekuneemesha kwa kukupa Unabii, si mchachefu wa akili, wala mpumbavu wa mawazo.

3 Na hakika unapata thawabu kubwa zisio katika kwa ajili ya kufikisha Ujumbe.

4 Na hakika wewe bila ya shaka umeshikamana na sifa nzuri kabisa na vitendo vizuri kabisa alivyo kuumba navyo Mwenyezi Mungu.

5 Karibuni hivi, ewe Muhammad, utaona, na makafiri wataona, ni nani kati yenu aliye mwenda wazimu.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Hakika Mola wako Mlezi, Yeye ndiye Mwenye kumjua zaidi aliye iacha Njia yake, na Yeye ndiye Mwenye kuwajua zaidi wenye akili walio ongoka kumwenda Yeye.

8 Basi usiyaache uliyo nayo ya kuwapinga wanao kanusha. Wanatamani lau ungeli kuwa laini kwao katika baadhi ya mambo, ili na wao wawe laini kwako, kwa tamaa upate kurudishiana nao. (Neno lililo tumiwa hapo "*Tud- hinu fayud-hinuun*", maana yake khasa "Upake mafuta na wao wapake mafuta". Kiswahili husema: Kumpaka mtu mafuta kwa mgongo wa chupa. Yaani kumpa sifa za uwongo, kumfanyia unaafiki. Kwa Kiarabu ni "*Mudaahana*". Kupakana mafuta)

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Wala usiache mwendo wako ulio nao kwenda kinyume na kila mwingi wa viapo, mtu wa kudharauliwa, mtapitapi mwenye kueneza aibu za watu, mwenye kuwasengenya watu, kuwasema kwa siri, mwenye

11. Mtapitapi, apitaye akifitini,¹¹
12. Mwenye kuzuia kheri, dhaalimu, mwingi wa madhambi,¹²
13. Mkavu, na juu ya hayo, mshari, amejipachika tu.¹³
14. Ati kwa kuwa ana mali na watoto!¹⁴
15. Anapo somewa Aya zetu, husema: Hizi ni simulizi za uwongo za watu wa zamani!¹⁵
16. Tutamtia kovu juu ya pua yake.¹⁶
17. Hakika tumewajaribu hawa kama tulivyo wajaribu wale wenye shamba, walipo apa kwamba watayavuna mazao yake itakapo kuwa asubuhi.¹⁷
18. Wala hawakusema: Mungu akipenda!¹⁸
19. Basi lilitokea tukio juu yake kutoka kwa Mola wako Mlezi, nao wamelala!¹⁹
20. Likawa kama usiku wa giza.²⁰
21. Asubuhi wakaitana.²¹
22. Ya kwamba nendeni kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna.²²
23. Basi walikwenda na huku wakinong'onezana,²³
24. Ya kuwa leo hata masikini mmoja asikuingilieni.²⁴
25. Na walikwenda asubuhi, nao wameshikilia azimio hilo.²⁵
26. Basi walipo liona, wakasema: Hakika tumepotea!²⁶
27. Bali tumenyimwa!²⁷
28. Mbora wao akasema: Sikukwambieni, kwa nini hamumtakasi Mwenyezi Mungu?²⁸
29. Wakasema: Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tulikuwa wenye

kutwaa maneno baina ya watu kwa sababu ya kuwafisidi, mwingi wa kupinga kila la kheri, dhaalimu, mwingi wa madhambi, mgumu wa moyo, mwenye tabia ya ukavu, muovu maarufu kwa shari, juu ya sifa hizo mbovu alizo nazo.

11 Tazama tanbihi ya 10.

12 Tazama tanbihi ya 10.

13 Tazama tanbihi ya 10.

14 Ati kwa kuwa anajiona yeye ana mali na watoto wengi! Amezikadhibisha Aya zetu na amezipuza. Akisomewa Qur'ani husema: Hivi ni visa vya uwongo vya watu wa kale!

15 Tazama tanbihi ya 14.

16 Tutambandika alama juu ya pua yake ya kumganda, apate kufedheheka mbele za watu.

17 Sisi tumewafanyia mtihani watu wa Makka kwa kuwapa neema, nao wakazikufuru; kama tulivyo wafanyia mtihani hao watu wenye shamba, walipo chukua kiapo kuwa watakwenda vuna mazao ya shamba lao asubuhi mapema, wala wasimkumbuke Mwenyezi Mungu, wakafunganisha hilo jambo lao na kupenda kwake.

18 Tazama tanbihi ya 17.

19 Basi ikaliteremkia shamba hilo balaa kubwa ilio toka kwa Mola wako Mlezi, na hali wao wamelala. Likawa hilo shamba kama usiku wa giza kwa masaiibu yalio lifikia.

20 Tazama tanbihi ya 19.

21 Asubuhi wakawa wanaitana: Amkeni mapema mwende kondeni kwenu kama mmeazimia kuvuna.

22 Tazama tanbihi ya 21.

23 Wakatoka, nao wakinong'ona kuambizana: Msimwachie masikini yeyote kuingilieni leo!

24 Tazama tanbihi ya 23.

25 Wakenda hapo asubuhi mpaka kwenye shamba lao, na azma yao ovu hiyo, na wao ni wenye uwezo kaamili wa kutenda hayo kwa kujigamba kwao.

26 Walipo liona limekuwa jeusi limeungua, walisema nao wamebabaika: Hakika sisi bila ya shaka tumepotea. Hili silo shamba letu! Bali ndilo shamba letu! Na sisi tumenyimwa!

27 Tazama tanbihi ya 26.

28 Alisema aliye kuwa muadilifu wao na mbora wao akiwalaumu: Sikukwambieni mlipo kuwa mnasemazana kuwanyima masikini, hebu hamumkumbuki Mwenyezi Mungu mkaicha niya yenu?

kudhulumu.²⁹

30. Basi wakakabiliana kulaumiana wao kwa wao.³⁰

31. Wakasema: Ole wetu! Tulikuwa tumeikiuka mipaka!³¹

32. Asaa Mola wetu Mlezi akatubadilishia lilio bora kuliko hili. Hakika sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi.³²

33. Namna hivi yanakuwa mateso, na bila ya shaka mateso ya Akhera ni makubwa zaidi, laiti wangu jua!³³

34. Hakika wachamngu watakuwa na Bustani za neema kwa Mola wao Mlezi.³⁴

35. Kwani tutawafanya Waislamu kama wakosefu?³⁵

36. Mna nini? Mnahukumu vipi?³⁶

37. Au mnacho kitabu ambacho ndani yake mnasoma?³⁷

38. Kuwa mtapata humo mnayo yapenda?³⁸

39. Au mnazo ahadi za viapo juu yetu za kufika Siku ya Kiyama ya kuwa hakika mtapata kila mnayo jihukumia?³⁹

40. Waulize: Ni nani miongoni mwao dhamini wa haya?⁴⁰

41. Au wanao washirika? Basi wawalete washirika wao wakiwa wanasema kweli.⁴¹

42. Siku utakapo wekwa wazi mudi, na wataitwa kusujudu, lakini hawataweza,⁴²

43. Macho yao yatainama chini, fedheha itawafunika. Na hakika walikuwa wakiitwa wasujudu walipo kuwa wazima -⁴³

44. Basi niache na wanao kadhibisha maneno haya! Tutawavutia kidogo kidogo kwa

29 Wakasema walipo rejea kwenye uwongozi wao: Tunamtakasa Mwenyezi Mungu kuwa katudhulumu kwa yaliyo tusibu. Hakika sisi wenyewe ndio tumejidhulumu kwa makusudio yetu maovu.

30 Wakawa wanaelekeana wao kwa wao wakilaumiana, wakisema: Huku ni kuhiliki kwetu! Hakika sisi tulikuwa tumepita mipaka katika dhulma zetu.

31 Tazama tanbihi ya 30.

32 Asaa Mola wetu Mlezi akatupa badala lilio bora kuliko hili shamba letu. Hakika sisi tunamtaka Mola wetu Mlezi peke yake atupe msamaha na malipo.

33 Mfano wa kama hayo yaliyo yasibu hilo shamba ndio inakuwa adhabu yangu ninayo iteremsha duniani kwa anaye stahiki. Na bila ya shaka adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi lau kuwa watu wanajua hayo.

34 Hakika wachamngu watapata kwa Mola wao Mlezi Bustani za neema safi.

35 Je! Sisi tudhulumu katika hukumu yetu, tuwafanye Waislamu sawa na makafiri? Nini lilio kusibuni nyinyi? Vipi mnahukumia mfano wa hukumu kama hii ya dhulma?

36 Tazama tanbihi ya 35.

37 Kwani mnacho kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu mnacho kisoma, na humo yamo hayo mnayo yapenda?

38 Tazama tanbihi ya 37.

39 Au kwani mnazo ahadi juu yetu zenye kutiliwa mkazo kwa viapo, zenye kubaki mpaka Siku ya Kiyama, kwamba mnayo haki ya hayo mnayo jihukumia?

40 Ewe Muhammad! Waulize washirikina: Ni nani dhamini wa hukumu hiyo?

41 Kwani wanao wanao shirikiana nao, na wanao fuata mwendo wao katika kauli yao hii? Basi na wawalete hao washirika wao, ikiwa wao ni wasema kweli katika madai yao.

42 Siku mambo yatapo shitadi na yakawa magumu, na wakatakiwa makafiri wasujudu kwa kuwaamea na kuwakejeli, na wasiweze, macho yao yameinama chini, yamefunikwa na fedheha. Na duniani walikuwa wakitakiwa wasujudu walipo kuwa wakiweza na wakakataa kusujudu. (Kuwekwa wazi mudi, ni kinaya ya kudhihirishwa kweli yote Siku ya kwima kondo, Siku ya Kiyama. Chambilecho Sayyid Abdulla bin Ali bin Nassir katika Al Inkishaf:

Tafakari siku ya kwima kondo, Ya kuaridhiwa kila kitendo, Pindi madhulumu atapo ondo, Achamba Ya Rabi namua naye).

43 Tazama tanbihi ya 42.

mahali wasipo pajua.⁴⁴

45. Na ninawapururia muhula; hakika hila zangu ni imara.⁴⁵

46. Au unawaomba ujira, na wao wanaemewa na gharama hiyo?⁴⁶

47. Au iko kwao siri, basi wao wanaiandika?⁴⁷

48. Basi ingojee hukumu ya Mola wako Mlezi, wala usiwe kama mmezwa na samaki, alipo nadi naye kazongwa.⁴⁸

49. Kama isingeli mfikia neema kutoka kwa Mola wake Mlezi, bila ya shaka angeli tupwa ufukweni naye ni mwenye kulaumiwa.⁴⁹

50. Lakini Mola wake Mlezi alimteua na akamfanya miongoni mwa watu wema.⁵⁰

51. Na walio kufuru hukaribia kukutelezesha kwa macho yao, wanapo sikia mawaidha, na wanasema: Hakika yeye ni mwendawazimu.⁵¹

52. Na hayakuwa haya, ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote.⁵²

44 Ewe Muhammad! Nachilie na hao wanao ikadhibisha Qur'ani. Tutawajongeza kwenye adhabu kidogo kidogo kwa jiha wasio ijua kuwa adhabu itatokea huko.

45 Na nitawapa muhula kwa kuiakharisha adhabu. Hakika mipango yangu ni ya nguvu, na hawezi kuporonyoka yeyote akasalimika nayo.

46 Kwani wewe unawaomba ujira kwa kuufikisha Ujumbe wako, na kwa hivyo wao wanaona uzito kwa gharama hiyo unayo wakalifisha?

47 Au kwani wao wanajua yaliyo fichikana na wao wanayaandika na ndio wanahukumu kwa hayo.

48 Basi wewe subiri kwa tunavyo wapa muhula na kukuakhirisha kukuletea manusura yetu juu yao. Wala usiwe kama Yunus, aliye mezwa na samaki, akawa na haraka na kuwaghadhibikia watu wake, alipo mnadia Mola wake Mlezi, naye kajaa hasira na ghadhabu, akitaka waadhibiwe kwa haraka.

49 Lau kuwa neema ya Mola wake Mlezi haikumdiriki kwa kukubali toba yake, angeli tupwa kutokana na tumbo la samaki ufukweni, naye akiteseka kwa kuteleza kwake.

50 Lakini Mola wake Mlezi kamteuwa kwa kuikubali toba yake, na akamjaalia miongoni mwa watu wema.

51 Na makafiri wangeli karibia kukutelezesha na pahala pako, kwa jicho lao wanalo kuangalia kwa uadui na chuki wanapo isikia Qur'ani, wakisema: Hakika huyu ni mwendawazimu.

52 Na Qur'ani si chochote ila ni mawaidha, na hikima, na ukumbusho kwa walimwengu wote.

Sura 69 - Al-H'aaqqah

Utangulizi

Sura hii tukufu inaeleza hali za Kiyama, na imetaja yaliyo wasibu watu wa mataifa yaliyo tangulia, ya kuteketezwa, na kuchukuliwa kwa nguvu na shida walipo kadhibisha. Na imetaja namna litavyo pulizwa baragumu, na mageuzi na kuondoka yatakayo zisibu ardhi na milima na mbingu. Na yatakayo tokea baada ya hayo ya kuletwa watu kwa ajili ya hisabu, na kubashiriwa watu wa mkono wa kulia kwa malipo ya ukarimu na neema za daima watakazo zipata, na maonyo ya watu wa kushoto na adhabu chungu. Tena Sura ikakhitimisha kwa kutaja ukweli wa Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. katika Ujumbe alio ufikisha, na ukweli wa Qur'ani ambao ndio ni Haki iliyo yakini.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Tukio la haki.¹
2. Nini hilo Tukio la haki?²
3. Na nini kitakujuulisha nini hilo Tukio la haki?³
4. Thamudi na A'di waliukadhibisha Msiba unao situsha.⁴
5. Basi Thamudi waliangamizwa kwa balaa kubwa mno.⁵
6. Na ama A'di waliangamizwa kwa upepo mkali usio zuilika.⁶
7. Alio wapelekea masiku saba, na siku nane, mfululizo bila ya kusita. Utaona watu wamepinduka kama kwamba ni magongo ya mitende yalio wazi ndani.⁷
8. Basi je! Unamwona mmoja wao aliye baki?⁸
9. Na Firauni na walio mtangulia, na miji iliyo pinduliwa chini juu, walileta khatia.⁹
10. Wakamuasi Mtume wa Mola wao Mlezi, ndipo Yeye Mola akawakamata kwa mkamato ulio zidi nguvu.¹⁰
11. Maji yalipo furika Sisi tulikupandisheni katika safina,¹¹

1 Kiyama ni Tukio litakalo tukia kwa haki, yaani kwa kweli. Ni nini hicho Kiyama kitacho tokea kweli?

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Na kitu gani kitacho kujuyva ukweli wake, na kitacho kupa sura ya kitisho chake na shida zake?

4 Kina Thamudi na kina A'di walikanusha Kiyama kinacho wagutua walimwengu wote kwa kitisho chake na shida zake.

5 Ama Thamudi basi walihilikiwa kwa tukio lilio pindukia mipaka yote kwa ukali wake.

6 Na ama A'di waliangamizwa kwa upepo ubaridi na mkali,

7 Mwenyezi Mungu aliwasalitisha nao muda wa masiku saba, na siku nane zilizo fuatana mfululizo, utaona walio patikana na upepo huo wamekuwa maiti kama magogo ya mitende yaliyo kuwa matupu ndani yake. ("Masiku" ni wingi wa "Usiku"; "Siku" wingi wake ni "Siku" vile vile.)

8 Je! Unamwona yeyote aliye bakia katika hao?

9 Akaja Firauni, na mataifa mengine yaliyo kufuru kabla yake, na wale jamaa walio acha mwendo wa haki na vitendo vya maumbile wakafanya vitendo vichafu kabisa hata miji yao ikapinduliwa juu chini.

10 Kila umma katika hawa walimuasi Mtume wa Mola wao Mlezi. Naye Mwenyezi Mungu akawashika kwa kuwaadhibu kwa mshiko ulio zidi ukali.

11 Maji yalipo zidi ukomo wake, na yakapanda juu ya milima katika tukio la tofani ya Nuhu, Sisi tulikupandisheni, yaani kwa kuwapandisha wazee wenu wa asli, katika safina inayo kwenda baharini.

12. Ili tuyafanye hayo kuwa ni waadhi kwenu na kila sikio linalo sikia liyahifadhi.¹²
13. Na litapo pulizwa barugumu mpulizo mmoja tu,¹³
14. Na ardhi na milima ikaondolewa, na ikavunjwa kwa mvunjo mmoja,¹⁴
15. Siku hiyo ndio Tukio litatukia.¹⁵
16. Na mbingu zitapasuka, kwani siku hiyo zitakuwa dhaifu kabisa.¹⁶
17. Na Malaika watakuwa pembezoni mwa mbingu; na wanane juu ya hawa watakuwa wamebeba Kiti cha Enzi cha Mola wako Mlezi.¹⁷
18. Siku hiyo mtahudhurishwa - haitafichika siri yoyote yenu.¹⁸
19. Basi ama atakaye pewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, atasema: Haya someni kitabu changu!¹⁹
20. Hakika nalijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu.²⁰
21. Basi yeye atakuwa katika maisha ya kupendeza,²¹
22. Katika Bustani ya juu,²²
23. Matunda yake yakaribu.²³
24. Waambiwe: Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya mlivyo tanguliza katika siku zilizo pita.²⁴
25. Na ama atakaye pewa kitabu chake katika mkono wake wa kushoto, basi yeye atasema: Laiti nisingeli pewa kitabu changu!²⁵
26. Wala nisingeli jua nini hisabu yangu.²⁶
27. Laiti mauti ndiyo yangeli kuwa ya kunimaliza kabisa.²⁷
28. Mali yangu hayakunifaa kitu.²⁸

12 Ili kulifanya tukio hilo la kuwaokoa Waumini na kuwazamisha makafiri liwe zingatia na mawaidha kwenu, na lihifadhiwe na kila sikio lenye kuhifadhi linalo sikia.

13 Litakapo pulizwa barugumu kwa mpulizo mmoja, na ardhi na milima ikaondolewa pahala ilipo, na ikavunjwa mara moja.

14 Tazama tanbihi ya 13.

15 Siku hiyo ndiyo kitashuka cha kushuka, na mbingu zitapasuka kwa kuondoka hukumu zake na sharia zake, kwani siku hiyo zitakuwa dhaifu baada ya kuwa madhubuti zenye nguvu.

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Na Malaika pembezoni mwake, na wapo Malaika wanane siku hiyo watakao beba Kiti cha Enzi cha Mola wako Mlezi, juu ya Malaika hawa wengine.

18 Siku hiyo ndio mtaletwa kwa ajili ya kuhisabiwa. Wala haifichikani siri yenu yoyote mliyo kuwa mkiificha.

19 Ama mwenye kupewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, atasema akiwatangazia furaha yake walio karibu naye: Chukueni msome kitabu changu!

20 Mimi nilikuwa na yakini tangu duniani kuwa nitapata hisabu yangu, basi nikajitayarisha nafsi yangu kwa mkutano huu.

21 Basi huyo atakuwa katika maisha yaliyo enea kupendeza.

22 Katika Bustani ya pahali na daraja ya juu.

23 Matunda yake yakaribu kwa kuyachuma. (kuyatunda).

24 Kuleni na mnywe kwa kula na kunywa kusio na karaha, wala maudhi, kwa sababu ya vitendo vyema mlivyo kwisha vitanguliza katika siku za duniani zilizo pita.

25 Ama mwenye kupewa kitabu chake kwa mkono wake wa kushoto atasema kwa majuto na huzuni: Laiti kuwa sikupewa kitabu changu, wala sikuijua hisabu yangu!

26 Tazama tanbihi ya 25.

27 Laiti kuwa kule kufa niliko kwisha kufa kungeli kuwa ndio kumalizika kwangu kwa mwisho, wala nisingeli fufuliwa tena!

28 Hapana chochote nilicho kimiliki duniani kilicho nifaa. Uzima wangu umenipotewa, na nguvu zangu zimitoka.

29. Madaraka yangu yamenipotea.²⁹
30. (Pasemwe): Mshikeni! Mtieni pingu!³⁰
31. Kisha mtupeni Motoni!³¹
32. Tena mtatizeni katika mnyororo wenye urefu wa dhira sabiini!³²
33. Kwani huyo hakika alikuwa hamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu,³³
34. Wala hahimizi kulisha masikini.³⁴
35. Basi leo hapa hana jamaa wa kumwonea uchungu,³⁵
36. Wala hana chakula ila usaha wa watu wa Motoni.³⁶
37. Chakula hicho hawakili ila wakosefu.³⁷
38. Basi naapa kwa mnavyo viona,³⁸
39. Na msivyo viona,³⁹
40. Kwa hakika hii ni kauli iliyo letwa na Mjumbe mwenye hishima.⁴⁰
41. Wala si kauli ya mtunga mashairi. Ni machache sana mnayo yaamini.⁴¹
42. Wala si kauli ya kuhani. Ni machache mnayo yakumbuka.⁴²
43. Ni uteremsho utokao kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.⁴³
44. Na lau kama angeli tuzulia baadhi ya maneno tu,⁴⁴
45. Bila ya shaka tungeli mshika kwa mkono wa kulia,⁴⁵
46. Kisha kwa hakika tungeli mkata mshipa mkubwa wa moyo!⁴⁶
47. Na hapana yeyote katika nyinyi ambaye angeli weza kutuzuia.⁴⁷

29 Tazama tanbihi ya 28.

30 Wataambiwa walinzi wa Jahannamu: Mshikeni, na mfungeni mikono yake kwenye shingo yake. Kisha msimtie popote ila ndani ya Moto wa Jahannamu, kisha mfungeni kwenye mnyororo mrefu kabisa.

31 Tazama tanbihi ya 30.

32 Tazama tanbihi ya 30.

33 Hakika huyo alikuwa hamsadiki Mwenyezi Mungu Mtukufu, wala hamhimizi yoyote kuwalisha masikini.

34 Tazama tanbihi ya 33.

35 Basi hii leo huyu kafiri hana jamaa wa kumtetea, wala hana chakula ila usaha wa watu wa Motoni, ambao kwa hakika ni mchanganyiko wa damu na usaha. Hawakili chakula hicho ila wakosefu walio kusudia kufanya maasi yao, na wakakamia kuendelea nayo.

36 Tazama tanbihi ya 35.

37 Tazama tanbihi ya 35.

38 Basi naapa kwa mnavyo viona katika vinavyo onekana, na msivyo viona katika ulimwengu wa ghaibu, kwamba hakika Qur'ani bila ya shaka inatoka kwa Mwenyezi Mungu kwa ulimi wa Mjumbe mwenye cheo cha juu.

39 Tazama tanbihi ya 38.

40 Tazama tanbihi ya 38.

41 Wala Qur'ani si maneno ya mtunga mashairi kama mnavyo dai. Ama nyinyi ni chache mno imani yenu ya kuwa Qur'ani inatoka kwa Mwenyezi Mungu.

42 Wala Qur'ani haisemi kwa maneno ya kumunyia munyia kama wananavyo makuhani mlio wazoea. Ni uchache mno kukumbuka kwenu na kuzingatia khitilafu zilioko baina ya Qur'ani na maneno ya makuhani.

43 Hii ni uteremsho unao toka kwa Mwenye kuwaangalia walimwengu wote kwa kuwaumba na kuwalea.

44 Na lau kuwa angeli dai kitu chochote ambacho tusicho kisema basi bila ya shaka tungeli mshika akitoe kama mtu anavyo mkamata mtu kwa mkono wa kulia akammaliza hapo hapo. Kisha bila ya shaka tungeli mkata mshipa wake wa moyo, afe saa ile ile. (Biblia inasema katika Kumbukumbu la Torati 18.20 "Lakini nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulina, au atakayenena katika jina la miungu mingine, nabii yule atakufa.")

45 Tazama tanbihi ya 44.

46 Tazama tanbihi ya 44.

47 Na hapana yeyote katika nyinyi, hata ange kuwa na nguvu namna gani, angeli weza kuzuia adhabu

48. Kwa hakika hii ni mawaidha kwa wachamngu.⁴⁸
49. Na hakika Sisi bila ya shaka tunajua kwamba miongoni mwenu wapo wanao kadhibisha.⁴⁹
50. Na hakika bila ya shaka itakuwa ni majuto kwa wanao kataa.⁵⁰
51. Na hakika hii bila ya shaka ni haki ya yakini.⁵¹
52. Basi litakase jina la Mola wako Mlezi Mtukufu.⁵²

yetu isimfikilie.

48 Na hakika Qur'ani ni mawaidha kwa wanao fuata amri za Mwenyezi Mungu, na wanaepuka makatazo yake.

49 Na hakika Sisi bila ya shaka tunajua kwamba kati yenu wapo wanao ikanusha Qur'ani.

50 Na kwamba hakika hiyo bila ya shaka ni sababu ya majuto ya wanao ikataa, wakati watapo iona adhabu yao, na neema za wenye kusadiki.

51 . Na hakika Qur'ani bila ya shaka ni Haki iliyo thibiti, isiyo na shaka yoyote.

52 Basi mtakase Mola wako Mlezi, na dumisha kudhukuru jina lake.

Sura 70 - Al-Maa'rij

Utangulizi

Katika Sura hii tukufu kipo kitisho kwa Siku ya Kiyama, na kutia khofu kwa urefu wake, na vitisho vikubwa vikubwa, na adhabu ambazo hazikubaliwi kutolewa fidia hata ya wana, wala mke, wala ndugu, wala ukoo mzima. Bali haikubaliwi fidia ya watu wa dunia nzima.

Na katika Sura hii unatolewa kombo udhaifu wa binaadamu wakati wa shida na neema, isipo kuwa aliye okolewa na Mwenyezi Mungu kwa uhamngu, na vitendo vyema. Hao wanasalimika na udhaifu huo.

Humo vile vile yanaelezwa kuchukiza tabia ya makafiri ya kuwa na tamaa ya uharibifu. Na mwishoni anausiwa Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. awawachilie mbali na upumbavu wao na mchezo wao mpaka wakutane na siku yao waliyo ahidiwa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayo tokea,¹
2. Kwa makafiri - ambayo hapana awezaye kuizuia -²
3. Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye mbingu za daraja.³
4. Malaika na Roho hupanda kwendea kwake katika siku ambayo kadiri yake ni miaka khamsini elfu!⁴
5. Basi subiri kwa subira njema.⁵
6. Hakika wao wanaiona iko mbali,⁶
7. Na Sisi tunaiona iko karibu.⁷
8. Siku ambayo mbingu zitakapo kuwa kama maadeni iliyo yayushwa.⁸
9. Na milima itakuwa kama sufi.⁹
10. Wala jamaa hatamuuliza jamaa yake.¹⁰

1 Ameita, mwenye kuita, kuhimiza kama kufanya kejeli, iletwe upesi adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambayo hapana shaka itawashukia makafiri. Wala hapana chochote cha kuzuia adhabu hiyo, kwani hiyo inatoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye mbingu, ambako huko ndiko zinatoka nguvu zinazo simama, na hukumu inayo tekelezwa.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Malaika na Jibrili wanapanda kwenda kunako toka amri yake kwa siku ambayo urefu wake ni miaka khamsini elfu kwa mujibu wa hisabu ya miaka ya duniani.

5 Basi, ewe Muhammad! Subiri uwastahamilie hizo kejeli zao, na kuhimiza kwao adhabu, kwa subira isiyo kuwa na mbabaiko ndani yake wala mashtaka. Hakika hao makafiri wanaiona hiyo Siku ya Kiyama ni kitu cha muhali kutokea. Na Sisi tunaona kuwa ni jambo jepesi katika uweza wetu, wala halina uzito wowote.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Tazama tanbihi ya 5.

8 Siku mbingu itakapo kuwa kama fedha iliyo yayuka, na milima itakapo kuwa kama sufi iliyo tiwa rangi na ikapigwa, wala jamaa hamuulizi jamaa yake: Nini hali yako? Kwa sababu kila mmoja kajishughulikia nafsi yake!

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Tazama tanbihi ya 8.

11. Ijapo kuwa wataonyeshwa waonane. Atatamani mkosefu lau ajikomboe na adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa fidia wanawe,¹¹
12. Na mkewe, na nduguye,¹²
13. Na jamaa zake walio kuwa wakimkimu,¹³
14. Na wote waliomo duniani, kisha aokoke yeye.¹⁴
15. La, hash! Kwa hakika huo ni Moto mkali kabisa,¹⁵
16. Unao babua ngozi ya kichwa!¹⁶
17. Utamwita kila aliye geuza mgongo na akageuka.¹⁷
18. Na akakusanya mali, kisha akayahifadhi.¹⁸
19. Hakika mtu ameumbwa na papara.¹⁹
20. Inapo mgusa shari hupapatika.²⁰
21. Na inapo mgusa kheri huizuilia.²¹
22. Isipo kuwa wanao sali,²²
23. Ambao wanadumisha Sala zao,²³
24. Na ambao katika mali yao iko haki maalumu²⁴
25. Kwa mwenye kuomba na anaye jizuilia kuomba;²⁵
26. Na ambao wanaisadiki Siku ya Malipo,²⁶
27. Na ambao wanaiogopa adhabu itokayo kwa Mola wao Mlezi.²⁷

11 Watakuwa wakijuulishana wao kwa wao mpaka wajuane baraabara, na ilhali hapana amuilizae mwenzie kitu. Kafiri atatamani lau ange pata kujikomboa nafsi yake na adhabu hiyo Siku ya Kiyama kwa kumtoa mwanawe awe ni fidia yake, au mkewe, au nduguye, au jamaa zake aliyo khusiana nao, na wote waliomo duniani, apate kuokoka yeye tu!

12 Tazama tanbihi ya 11.

13 Tazama tanbihi ya 11.

14 Tazama tanbihi ya 11.

15 Ewe mkosefu! Wacha hayo unayo yatamani ya kutaka kujikomboa kwa fidia! Hakika huo moto, unawaka kweli! Utakubabua mikono yako, na miguu yako, na viungo vyako vyote, utanadi kwa jina la huyo aliye iacha Haki, na akaacha ut'iifu, na akakusanya mali akayaweka katika mabweta yake, wala hakutoa haki ya Mwenyezi Mungu iliomo katika hayo mali!

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Tazama tanbihi ya 15.

18 Tazama tanbihi ya 15.

19 Hakika tabia ya binaadamu ni papara, mwingi wa kupapatika, na kutoridhika akifikiwa na lolote la karaha na uzito, na ni mwingi wa kuzuia na kunyima akipata kheri na neema. Isipo kuwa wanao sali, ambao wanadumisha Sala zao, hawakikosi hata kipindi kimoja. Hao Mwenyezi Mungu huwakinga, na huwawezesha kutenda yaliyo kuwa ya kheri.

20 Tazama tanbihi ya 19.

21 Tazama tanbihi ya 19.

22 Tazama tanbihi ya 19.

23 Tazama tanbihi ya 19.

24 Na wale ambao katika mali yao ipo haki iliyo ainiwa iliyo wekwa kwa ajili ya masikini mwenye kuomba kutaka msada, na anaye jizuilia kuomba pia. (Katika wanao zuilika kuomba wanaingia si wenye kustahi na kuona vibaya tu, bali pia wasio weza kuomba kama watoto wachanga, wagonjwa, na wanyama pia.)

25 Tazama tanbihi ya 24.

26 Na wale wanao isadiki Siku ya Malipo, basi wanajitayarisha kwa ajili yake; na wale wanao iogopa adhabu ya Mola wao Mlezi basi wanajikinga nayo wala hawajitii katika jambo la kuwaletea adhabu hiyo. Kwani hakika adhabu ya Mola wao Mlezi hapana hata mmoja anaye weza kuaminika nayo isimpate.

27 Tazama tanbihi ya 26.

28. Hakika adhabu ya Mola wao Mlezi si ya kuaminika nayo.²⁸
29. Na ambao wanahifadhi tupu zao.²⁹
30. Isipo kuwa kwa wake zao, au iliyo wamiliki mikono yao ya kuume, basi hao hawalaumiwi.³⁰
31. Lakini wanao taka kinyume ya haya, basi hao ndio wanao ruka mipaka.³¹
32. Na ambao wanazichunga amana zao na ahadi zao,³²
33. Na ambao wanasimama imara katika ushahidi wao,³³
34. Na ambao wanazihifadhi Sala zao.³⁴
35. Hao ndio watakao hishimiwa Peponi.³⁵
36. Wana nini wale walio kufuru wanakutumbulia macho tu?³⁶
37. Makundi kwa makundi upande wa kulia na upande wa kushoto!³⁷
38. Kwani kila mmoja wao anatumai kuingizwa katika Pepo ya neema?³⁸
39. La, hash! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na wanacho kijua.³⁹
40. Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mashariki zote na magharibi zote kwamba Sisi tunaweza⁴⁰
41. Kuwabadili kwa walio bora kuliko wao; na Sisi hatushindwi.⁴¹
42. Basi waache wapige porojo na wacheze, mpaka wakutane na siku yao wanayo ahidiwa,⁴²
43. Siku watakapotoka makaburini kwa upesi kama kwamba wanakimbilia mfundo,⁴³

28 Tazama tanbihi ya 26.

29 Na ambao wanazihifadhi tupu zao hata hawaemewi na matamano yao. Lakini kwa wake zao na masuria wao hawazihifadhi; kwa sababu hapo hawalaumiwi kuifuata tabia ya maumbile. Basi mwenye kutafuta starehe ya maingiliano kwa wasio kuwa wake na masuria, basi hao tena ni wenye kuikiuka halali na kuingia katika haramu.

30 Tazama tanbihi ya 29

31 Tazama tanbihi ya 29.

32 Na hao wenye kuzihifadhi amana za sharia na amana za waja wa Mwenyezi Mungu, na walio lazimika nayo kwa Mwenyezi Mungu na kwa watu bila ya kukhuni wala kupunja, na ambao kwa shahada zao wamesimama sawa sawa kwa haki bila ya kuficha wanalo lijua, na wanao hifadhi Sala zao wakizisali sawasawa kwa ukamilifu-

33 Tazama tanbihi ya 32.

34 Tazama tanbihi ya 32.

35 Watu wenye sifa kama hizo nzuri watakuwa ni wenye kuhishimiwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu huko Peponi.

36 Kitu gani kinawapelekea hao walio kufuru kukujia mbio mbio kutoka kuliani na kushotoni kwa makundi? Je, kwani kila mmoja wao ana tamaa ya kuingia kwenye Pepo yenye neema, baada ya kusikia kuwa Mwenyezi Mungu amemuahidi Mtume wake na Waumini kuwatia Peponi?

37 Tazama tanbihi ya 36.

38 Tazama tanbihi ya 36.

39 Basi nawaache hiyo tamaa yao ya kuingia Peponi. Hakika Sisi tumewaumba wao kutokana na maji ya kudharauliwa.

40 Naapa kwa Mola Mlezi wa mashariki zote, na magharibi zote za siku, na sayari na hidaya, kwamba hakika bila ya shaka Sisi tuna uweza wa kuwaangamiza, na kuwaleta walio wat'ifu zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko wao. Wala Sisi hatushindwi kubadilisha huko. (*Tazama Maelezo 70:40*)

41 Tazama tanbihi ya 40.

42 Basi waachilie wakiporojoka katika upotovu wao, na wakicheza na dunia yao, mpaka wakutane na siku yao waliyo ahidiwa kupewa adhabu.

43 Siku watakapo tolewa makaburini mbio mbio kumwenda huyo ataye waita, kama kwamba wamemweka ufundo na wakimuabudu duniani walivyo kuwa wakimkimbilia badala ya Mwenyezi Mungu, macho yameinama chini, hawawezi kuyanyanyua, yamegubikwa na unyonge na udhalili. Hiyo

44. Macho yao yatainama, fedheha itawafunika. Hiyo ndiyo Siku waliyo kuwa wakahidiwa.⁴⁴

ndiyo siku waliyo kuwa wakahidiwa duniani na wao wakiikanusha.

44 Tazama tanbihi ya 43.

Sura 71 - Nuh'

Utangulizi

Sura hii tukufu imefafanua kisa cha Nuh'u a.s. pamoja na kaumu yake. Ikasimulia khabari za wito wake kwa dhaahiri, kisha kwa siri na kwa dhaahiri. Na ikaeleza mashtaka yake kumshtakia Mwenyezi Mungu juu ya walivyo mpuuza, na inda walio mfanyia, na ikasajili kukakamia kwao kuyaabudu masanamu mpaka wakastahiki kupata adhabu ya Mwenyezi Mungu. Nuh'u alipo kata tamaa nao kuukubali wito wake, aliwaapiza wahiliki na waangamie, na akajiombea nafsi yake, na wanawe, Waumini wanaume, na Waumini wanawake, wapate msamaha.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Hakika Sisi tulimtuma Nuh'u kwa watu wake: Uwaonye kaumu yako kabla ya kuwafikia adhabu chungu.¹
2. Akasema: Enyi watu wangu! Kwa hakika mimi ni mwonyaji wa dhaahiri kwenu,²
3. Ya kwamba mumuabudu Mwenyezi Mungu, na mumche Yeye, na mumt'ii.³
4. Atakughufirieni madhambi yenu, na atakuakhirisheni mpaka muda ulio wekwa. Hakika muda wa Mwenyezi Mungu utapo fika haucheleweshwi. Laiti mngejua!⁴
5. Akasema: Ee Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimewaita watu wangu usiku na mchana,⁵
6. Lakini wito wangu haukuwazidisha ila kukimbia.⁶
7. Na hakika mimi kila nilipo waita ili upate kuwaghufiria, walijiziba masikio yao kwa vidole vyao, na wakajigubika nguo zao, na wakakamia, na wakatakabari vikubwa mno!⁷
8. Tena niliwaita kwa uwazi,⁸

1 Hakika Sisi tulimtuma Nuh'u kwa watu wake, na tukamwambia: Waonye watu wako kabla haijawajia adhabu yenye machungu makali.

2 Nuh'u akasema: Enyi watu wangu! Hakika mimi ni mwonyaji kwenu, nina risala kutoka kwa Mola wenu Mlezi kwa lugha mnayo ijua, ya kwamba mumt'ii Mwenyezi Mungu, na mumnyenyekee katika kutimiza waajibu zote; na mwogopeni Yeye kwa kuacha mnayo katazwa, na nit'iini mimi katika ninayo kunasihini. Ndipo Mwenyezi Mungu atapo kusameheni madhambi yenu, na atakupeni umri mrefu mpaka ifike ajali iliyo wekwa mwisho wa umri wenu. Hakika mauti yakija hayaakhirishwi kabisa! Lau kuwa mngeli jua majuto mtakayo kuwa nayo utapo kwisha muda wenu mngeli amini.

3 Tazama tanbihi ya 2.

4 Tazama tanbihi ya 2.

5 Nuh'u akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimewaita watu wangu waumini usiku na mchana bila ya kuchoka, hawakuzidishwa na wito wangu ila kuukimbia ut'iifu wako.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Na mimi kila nikiwataka wakuamini Wewe upate kuwasamehe, hubandika vidole vyao kwenye masikio yao ili wasisikie wito wangu, na hujifunika kwa maguo yao ili wasiuone uso wangu! Na wakasimama kidete juu ya ukafiri wao, na wakatakabari kutakabari kukubwa mno!

8 Kisha nikawaita waje kwako kwa sauti ya juu, kisha nikaudhihirisha wito kwa namna moja, na nikawaita kisirisiri kwa namna nyengine, ili nijaribu kila njia.

9. Kisha nikawatangazia kwa kelele, tena nikasema nao kwa siri.⁹
10. Nikasema: Ombeni msamaha kwa Mola wenu Mlezi; hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe.¹⁰
11. Atakuleteeni mvua inyeshe mfululizo.¹¹
12. Na atakupeni mali na wana, na atakupeni mabustani na atakufanyieni mito.¹²
13. Mna nini hamweki heshima ya Mwenyezi Mungu?¹³
14. Na hali Yeye kakuumbeni daraja baada ya daraja?¹⁴
15. Kwani hamwoni jinsi Mwenyezi Mungu alivyo ziumba mbingu saba kwa matabaka?¹⁵
16. Na akaufanya mwezi ndani yake uwe nuru, na akalifanya jua kuwa taa?¹⁶
17. Na Mwenyezi Mungu amekuotesheni katika ardhi kama mimea.¹⁷
18. Kisha atakurudsheni humo na atakutoeni tena.¹⁸
19. Na Mwenyezi Mungu amekukunjulieni ardhi kama busati.¹⁹
20. Ili mtembee humo katika njia zilizo pana.²⁰
21. Nuh'u akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika hao wameniasi, na wamemfuata yule ambaye mali yake na wanawe hawakumzidishia ila khasara.²¹
22. Na wakapanga vitimbi vikubwa.²²
23. Na wakasema: Msiwaache miungu yenu, wala msimwache Wadda wala Suwaa' wala Yaghutha, wala Yau'qa, wala Nasra.²³

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Nikawambia watu wangu: Takeni kwa Mola wenu Mlezi maghfira kwa kufu zenu na maasi yenu. Kwani Yeye bado ni Mwingi wa kusamehe madhambi ya mwenye kurejea kwake. Atakuleteeni mawingu yatakayo miminika mvua kwa wingi, na atakupeni mali na wana, na hayo ndiyo mapambo ya dunia, na atakupeni mashamba mtayo starehea kwa uzuri wake na matunda yake, na atakujaalieni mito ya kunyweshea mazao yenu na mifugo yenu.

11 Tazama tanbihi ya 10.

12 Tazama tanbihi ya 10.

13 Mna nini nyinyi hata hamumtukuzi Mwenyezi Mungu kama anavyo stahiki kutukuzwa, ili mtaraji akukirimuni kwa kukuokoeni na adhabu, na hali Yeye ndiye aliye kuumbeni kwa madaraja, tangu tone ya manii, kisha pande la damu, kisha pande la nyama, kisha mafupa na nyama?

14 Tazama tanbihi ya 13.

15 Kwani huoni vipi Mwenyezi Mungu alivyo ziumba mbingu saba, moja juu ya moja, na akaufanya mwezi katika mbingu hizo unatoa nuru, na akalifanya jua ni taa ambayo kwayo watu wa duniani ndio wanaona kwa mwangaza wake yote wanayo hitajia kuyaona?

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni kutokana na ardhi, akakuotesheni kama miema kwa njia ya ajabu, kisha baada ya kufa atakurejesheni huko huko kwenye ardhi, na tena atakutoeni huko kwa hakika hapana hivi wala hivi.

18 Tazama tanbihi ya 17.

19 Na Mwenyezi Mungu ameifanya ardhi iliyo kunjuliwa ili mpate kwenda humo katika njia zenye wasaa.

20 Tazama tanbihi ya 19.

21 Alisema Nuh'u: Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikatalia mimi niliyo waamrisha ya kuamini na kutaka msamaha, na wakawafuata madhaifu miongoni mwao ambao mali yao na watoto wao hawawazidishii ila khasara tupu katika Akhera. Na vitimbi vya hao wenye mali mengi, na wana wengi, kwa wanyonge wanao wafuata ni vitimbi vilivyo fika ukomo kwa ukubwa.

22 Tazama tanbihi ya 21.

23 Na wao wakiwaambia: Msiache kuiabudu miungu yenu, wala msimwache Wadda, wala Suwaa', wala Yaghutha, wala Yau'qa, wala Nasra. Na hawa walikuwa miungu ya masanamu iliyo chongwa kwa sura ya wanyama namna mbali mbali. Na miungu hii iliwapoteza watu wengi. Na wala huwazidishii wenye kuzidhulumu nafsi zao kwa ukafiri na inda, ili kuzidi kubaidika na Haki.

24. Na hao walikwisha wapoteza wengi, wala usiwazidishie walio dhulumu ila kupotea.²⁴
25. Basi kwa ajili ya makosa yao waligharikishwa wakaingizwa Motoni, wala hawakuwapata wa kuwanusuru badala ya Mwenyezi Mungu.²⁵
26. Na Nuh'u akasema: Mola wangu Mlezi! Usimwache juu ya ardhi mkaazi wake yeyote katika makafiri!²⁶
27. Hakika ukiwaacha watawapoteza waja wako, wala wao hawatazaa ila waovu makafiri.²⁷
28. Mola wangu Mlezi! Nighufirie mimi na wazazi wangu, na kila aliye ingia nyumbani mwangu kuwa ni mwenye kuamini, na Waumini wote wanaume, na Waumini wanawake. Na wala usiwazidishie walio dhulumu ila kupotea.²⁸

24 Tazama tanbihi ya 23.

25 Kwa sababu ya madhambi yao wakazamishwa kwa tofani, na baada ya kuangamizwa kwao wakatiwa Motoni kwenye moto mkali wa kuwaka na kuteketeza, na wala wasipate yeyote baada ya kumkosa Mwenyezi Mungu, wa kuwanusuru na kuwakinga na adhabu!

26 Na Nuh'u akasema baada ya kukata tamaa nao watu wake: Mola wangu Mlezi! Usimwache yeyote katika hao wanao kukataa Wewe akabaki akizunguka juu ya ardhi!

27 Ewe Mola wangu Mlezi! Ukiwaacha hao bila ya kuwateketeza na kuwang'oa watawatia waja wako katika upotovu, na wao hawatozaa ila wenye kupotoka vile vile wakaiacha haki, na wakakithiri kukukanya na kukuasi.

28 Mola wangu Mlezi! Nisamehe mimi na wazazi wangu ambao ndio walio kuwa ni sababu ya kuzaliwa mimi, na kila mwenye kuingia nyumbani kwangu kwa kukuamini Wewe, na uwasamehe Waumini wote wanaume na wanawake. Na usiwazidishie makafiri ila kuwaangamiza.

Sura 72 - Al-Jinn

Utangulizi

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuamrisha Mtume wake s.a.w. katika Sura hii tukufu awafikishie watu aliyo funuliwa yeye kwa wahyi, kwamba majini wameisikiliza Qur'ani na wameitikia wito wake, na kuwapa khabari kwa yaliyo wapata wapumbavu wao na wema wao, na yaliyo kuwa kutokana na kukaa kwao kusikiliza kwa wizi, na kufukuzwa kwao hivi sasa. Na Aya za Sura hii zinaeleza khabari za hao wanao nyatia kwenye njia ya Uislamu na kuupinga, na ikasimulia juu ya kuisafishia misikiti kwa ajili ya kumuabudu Mwenyezi Mungu tu peke yake, na juu ya wito wa Mtume kumwendea Mwenyezi Mungu, na majini kumzunguka Mtume, na ikaeleza kwa kuwekea mipaka lipi aliwezalo Mtume na lipi ambalo haliwezi, na ikahadhirisha wenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume watahadhari na Jahannamu na kubakia humo milele. Na mwisho Sura ikakhitimisha kwamba Mwenyezi Mungu peke yake ndiye aliye khusika na kujua ilimu ya ghaibu, mambo yasiyo onekana, na humdokezea anaye mteuwa katika viumbe ili awe ni Mtume wa kuuhifadhi Wahyi kwa kuulinda mpaka awafikishie watu kwa utimilivu. Na Mwenyezi Mungu anayajua hayo

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza, na likasema: Hakika sisi tumeisikia Qur'ani ya ajabu!¹
2. Inaongoza kwenye uwongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yeyote na Mola wetu Mlezi.²
3. Na kwa hakika utukufu wa Mola wetu Mlezi umetukuka kabisa; hana mke wala mwana.³
4. Na kwa hakika wapumbavu miongoni mwetu walikuwa wakisema uwongo ulio pindukia mipaka juu ya Mwenyezi Mungu.⁴
5. Nasi tulidhani kuwa watu na majini hawamzulia uwongo Mwenyezi Mungu.⁵
6. Na hakika walikuwako wanaume katika watu walio kuwa wakitafula kujikinga kwa wanaume wa kijini; kwa hivyo wakawazidisha madhambi.⁶

1 Ewe Muhammad! Waambie watu wako: Nimepata wahyi kwamba kikundi cha majini kimesikia kusoma kwangu Qur'ani, nao wakawaambia wenzao: Hakika sisi tumeisikia Qur'ani ya namna ya peke yake, hatujapata kusikia mfano wake kabla yake, inaitia kwenye uwongofu na usawa. Kwa hivyo tumeiamini hiyo Qur'ani tuliyo isikia; na kabisa hatutamshirikisha Mola wetu Mlezi aliye tuumba na kutulea na chochote katika waja wake.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Na kwamba hakika cheo na utukufu wa Mola wetu Mlezi umetukuka; hana mke wala mwana.

4 Na hakika wajinga katika sisi walikuwa wakimzulia Mwenyezi Mungu maneno yaliyo kuwa mbali kabisa na ukweli na kuwa sawa.

5 Na hakika sisi tulikuwa tunadhani kuwa haiwi binaadamu au jini kumzulia Mwenyezi Mungu jambo ambalo si laiki naye kusifika nalo

6 Na walikuwako wanaume katika wanaadamu wakitafula ulinzi kwa wanaume wa kijini. Basi hao binaadamu hawakuwazidishia majini ila kuzidi uasi na ujinga na ujeuri.

7. Na kwa hakika wao walidhani, kama mlivyo dhani nyinyi, ya kuwa Mwenyezi Mungu hatamleta Mtume.⁷
8. Nasi tulizigusa mbingu, na tukazona zimejaa walinzi wenye nguvu na vimondo.⁸
9. Na hakika tulikuwa tukikaa humo katika baadhi ya makao ili kusikiliza; lakini sasa anaye taka kusikiliza atakuta kimondo kinamvizia!⁹
10. Nasi hatujui kama wanatakiwa shari wale wanao kaa kwenye ardhi au Mola wao Mlezi anawatakia uwongofu.¹⁰
11. Na hakika katika sisi wamo walio wema, na wengine wetu ni kinyume na hivyo. Tumekuwa njia mbali mbali.¹¹
12. Nasi tulijua kuwa hatutomshinda Mwenyezi Mungu duniani, wala hatuwezi kumponyoka kwa kukimbia.¹²
13. Nasi tulipo usikia uwongofu tuliuamini. Basi mwenye kumuamini Mola wake Mlezi basi haogopi kupunjwa wala kudhulumiwa.¹³
14. Na hakika wamo katika sisi Waislamu, na wamo kati yetu wanao acha haki. Basi walio silimu, hao ndio walio tafuta uwongofu.¹⁴
15. Na ama wanao acha haki, hao watakuwa kuni za Jahannamu.¹⁵
16. Na lau kama wangeli simama sawasawa juu ya njia tungeli wanyweshwa maji kwa wingi,¹⁶
17. Ili tuwajaribu kwa hayo. Na anaye puuza kumkumbuka Mola wake Mlezi atamsukuma kwenye adhabu ngumu.¹⁷
18. Na hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu.¹⁸
19. Na hakika Mja wa Mwenyezi Mungu alipo simama kumwomba, wao walikuwa

7 Na hakika majini walidhani, kama mlivyo dhani nyinyi, enyi binaadamu, kwamba Mwenyezi Mungu hatamfufua yeyote baada ya kwisha kufa, wala hatowaletea watu Mtume yeyote wa kibinaadamu.

8 Na hakika sisi tulitaka kufikilia mbinguni, tukakuta kumejaa walinzi wa kimalaika wenye nguvu, na vimondo vinavyo unguza kutoka upande huo.

9 Na sisi kabla ya leo tulikuwa tukikaa pande za mbinguni kwenye makao kwa ajili ya kuchunguza khabari za mbinguni. Lakini sasa mwenye kutaka kusikiliza anakuta vimondo vinamngojea kumzuia na kumtekeza.

10 Na hakika sisi hatujui imekusudiwa adhabu kwa walioko katika ardhi kwa huku kulindwa mbingu hata ikazuiliwa kusikilizwa, au Mola wao Mlezi anawatakia kheri na uwongofu?

11 Na hakika miongoni mwetu wapo walio wema wachamngu, na miongoni mwetu pia wapo walio kinyume na hivyo. Na hao ni walio wastani katika wema wao. Kwa hivyo sisi ni wa makundi mbali mbali.

12 Na hakika sisi tumeyakinika kwamba hatutamshinda Mwenyezi Mungu popote tutapo kuwapa katika ardhi, wala hatutamshinda hata tukifanya tuikimbie hukumu yake kwendea mbinguni.

13 Na hakika sisi tulipo isikia Qur'ani tuliiamini. Na mwenye kumuamini Mola wake Mlezi basi hachelei kupunguziwa chochote katika mema yake, wala kudhulumiwa kwa kuzidishiwa maovu yake.

14 Na hakika kati yetu wapo Waislamu wenye kuikubali Haki, na miongoni mwetu wapo wenye kuiacha njia ya uwongofu. Basi wenye kusilimu hao wameifuata njia ya Haki, na ni wenye kufanya jitihada katika kuikhiari njia hiyo.

15 Ama majeuri walio iacha njia ya Uislamu basi hao watakuwa ndio kuni za Jahannamu.

16 Na hakika lau kuwa watu na majini wakifuata Njia ya Uislamu, wala wasende upogo wakaiwacha, basi bila ya shaka tutawanyweshwa maji mengi yatakayo enea nyakati za haja.

17 Ili tuwajaribu tuwaone vipi watavyo mshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema anazo waneemesha. Na mwenye kukengeuka na ibada ya Mola wake Mlezi atamtia katika adhabu ya mashaka asiyo yaweza kuyachukua.

18 Na imefunuliwa kwangu kwamba kwa hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu peke yake. Basi msimuabudu yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu.

karibu kumzonga!¹⁹

20. Sema: Hakika mimi namwomba Mola wangu Mlezi, wala simshirikishi Yeye na yeyote.²⁰

21. Sema: Mimi sina mamlaka ya kukudhuruni wala kukuongozeni.²¹

22. Sema: Hakika hapana yeyote awezae kunilinda na Mwenyezi Mungu, wala sitapata pa kukimbilia isipo kuwa kwake Yeye tu.²²

23. Ila nifikishe Ujumbe utokao kwa Mwenyezi Mungu na risala zake. Na wenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi hakika hao watapata Moto wa Jahannamu wadumu humo milele.²³

24. Hata watakapo yaona wanayo ahidiwa, ndipo watakapo jua ni nani mwenye msaidizi dhaifu, na mchache wa idadi.²⁴

25. Sema: Sijui kama yapo karibu hayo mnayo ahidiwa, au Mola wangu Mlezi atayawekea muda mrefu.²⁵

26. Yeye ndiye Mwenye kujua ya siri, wala hamdhihirishii yeyote siri yake,²⁶

27. Isipo kuwa Mtume wake aliye mridhia. Naye huyo humwekea walinzi mbele yake na nyuma yake.²⁷

28. Ili Yeye ajue kwamba wao wamefikisha ujumbe wa Mola wao Mlezi, na Yeye anayajua vyema yote walio nayo, na amedhibiti idadi ya kila kitu.²⁸

19 Na imefunuliwa kwangu kwamba alipo simama Mja wa Mwenyezi Mungu, Muhammad, katika Sala yake akimuabudu Mwenyezi Mungu, majini walijikusanya makundi kwa makundi, wakistaajabu kwa waliyo kuwa wakiyaona na wakiyasikia.

20 Sema: Hakika mimi namuabudu Mola wangu Mlezi peke yake, wala simshirikishi na yeyote katika ibada.

21 Sema: Mimi sina uweza wowote juu yenu wa kukuondoleeni madhara, wala kukuleteeni uwongofu na manufaa.

22 Sema: Hakika mimi hapana yeyote awezae kuniondolea adhabu nikimuasi Mwenyezi Mungu. Wala sipati pa kukimbilia, kuikimbia adhabu yake.

23 Lakini niliwezalo ni kufikisha Ujumbe wa Mwenyezi Mungu na Risala zake alizo nituma nizifikishe. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akaipuuza Dini ya Mwenyezi Mungu, basi hakika mtu huyo atapata Moto wa Jahannamu abakie humo milele.

24 Hata watakapo iona adhabu waliyo ahidiwaa, hapo basi watajua wakati itapo shuka, nani mwenye msaidizi dhaifu na nguvu, na yupi mchache wa idadi. Ni wao au Waumini?

25 Sema: Enyi makafiri! Sijui ni karibu hiyo adhabu mliyo ahidiwa, au Mola wangu Mlezi ataifanya iwe mbali?

26 Yeye ndiye Mjuzi wa ghaibu, yaliyo siri. Hapana mmoja katika viumbe vyake anaye ijua siri yake, ila Mtume aliye mridhia kumjuvya baadhi ya hiyo siri. Naye humwekea mbele ya huyo Mtume na nyuma yake Malaika wa kumkinga na wasiwasi.

27 Tazama tanbihi ya 26.

28 Ili Mwenyezi Mungu ayajue hayo yametokea kwa kuwafikiana na alivyo kadiria, ya kwamba Manabii hakika wamefikisha Risala za Mola wao Mlezi. Na kwa hakika Yeye kesho jua kwa kufananua yote waliyo nayo, na anajua idadi ya viumbe vyote. Hapana kitu kinacho mpotea Yeye.

Sura 73 - Al-Muzzammil

Utangulizi

Katika Sura hii Mwenyezi Mungu amemuamrisha Mtume wake asimame sehemu kubwa ya usiku kwa ajili ya Sala na kusoma Qur'ani kwa utulivu. Akawa anasimama yeye na kikundi cha wale walio kuwa pamoja naye. Kisha Mwenyezi Mungu aliwapunguzia na akawaamrisha Sala, na Zaka, na Sadaka, na Kuomba maghfira.

Na miongoni ya hayo akamuamrisha avumilie kwa wayasemayo wale wanao kadhibisha, na awaachilie iwapate adhabu aliyo waahidi Mwenyezi Mungu; na Yeye amewaonya makafiri kwa mfano wa adhabu iliyo mshukia Firauni na walio kuwa pamoja naye, walipo muasi Mtume wa Mola wao Mlezi, na akawakhofisha kwa vitisho vya Kiyama.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ewe uliye jifunika!¹
2. Kesha usiku kucha, ila kidogo tu!²
3. Nusu yake, au ipunguze kidogo.³
4. Au izidishe - na soma Qur'ani kwa utaratibu na utungo.⁴
5. Hakika Sisi tutakuteremshia kauli nzito.⁵
6. Hakika kuamka usiku kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno yake yanatua zaidi.⁶
7. Kwani hakika mchana una shughuli nyingi.⁷

1 Ewe uliye jigubika kwa nguo zako! Inuka kwa ajili ya Sala usiku kucha, ila kidogo tu! Simama nusu ya usiku, au punguza kidogo katika hiyo nusu mpaka ifikie thuluthi, au zidisha kwenye nusu mpaka ifikie thuluthi mbili. Na soma Qur'ani kwa pole pole ukibainisha harufi, na pa kusita usite, pasiwe na nuksani yoyote.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Tazama tanbihi ya 1.

5 Ewe Mtume! Hakika Sisi tutakuteremshia Qur'ani yenye kukusanya amri, na makatazo, na takalifu nzito nzito.

6 Hakika ibada zinazo fanywa usiku zinaganda zaidi katika moyo wa mtu, na zinabainika zaidi ulimini, na zinasibu vyema zaidi, kuliko visomo vya ibada za mchana.

7 Hakika mchana unakuwa na mambo mengi ya kukuhangaisha kutafuta maslaha ya maisha yako, na kushughulika na mambo ya kufikisha Ujumbe. Basi jiwekee nafsi yako faragha ya usiku kwa ajili ya kumuabudu Mola wako Mlezi.

8. Na lidhukuru jina la Mola wako Mlezi, na ujitolee kwake kwa ukamilifu.⁸
9. Mola Mlezi wa mashariki na magharibi, hapana mungu isipo kuwa Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa wako.⁹
10. Na vumilia hayo wayasemayo, na jitenge nao kwa vizuri.¹⁰
11. Na niache Mimi na hao wanao kanusha, walio neemeka; na wape muhula kidogo!¹¹
12. Hakika Sisi tunazo pingu nzito na Moto unao waka kwa ukali kabisa!¹²
13. Na chakula kinacho kwama kooni, na adhabu inayo umiza.¹³
14. Siku ambayo ardhi itatikiswa na milima pia, na milima itakuwa kama tifutifu la mchanga!¹⁴
15. Hakika Sisi tumemtuma kwenu Mtume aliye shahidi juu yenu, kama tulivyo mtuma Mtume kwa Firauni.¹⁵
16. Lakini Firauni alimuasi huyo Mtume, basi tukamshika mshiko wa mateso.¹⁶
17. Basi nyinyi mkikufuru, mtawezaje kujikinga na Siku ambayo itawafanya watoto wadogo waote mvi?¹⁷
18. Hapo mbingu zitapasuka! Ahadi yake itakuwa imetekelezwa.¹⁸
19. Kwa hakika hili ni kumbusho. Mwenye kutaka atashika njia ya kwendea kwa Mola wake Mlezi.¹⁹
20. Hakika Mola wako Mlezi anajua ya kuwa hakika wewe unakesha karibu na thuluthi mbili za usiku, na nusu yake, na thuluthi yake. Na baadhi ya watu walio pamoja nawe kadhaalika. Na Mwenyezi Mungu ndiye anaye ukadiria usiku na mchana. Anajua kuwa hamwezi kuweka hisabu, basi amekusameheni. Basi someni kilicho chepesi katika Qur'ani. Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa, na wengine wanasafiri katika ardhi wakitafuta fadhila ya Mwenyezi Mungu, na wengine wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo someni kilicho chepesi humo, na mshike Sala, na toeni Zaka, na mkopesheni Mwenyezi Mungu mkopo mwema. Na kheri yoyote

8 Na pitisha ulimini mwako kudhukuru jina la Mola aliye kuumba na kukulea, na mkhusishe Yeye tu kwa ibada kwa ukamilifu.

9 Yeye ndiye Mwenye kumiliki mashariki na magharibi, hapana wa kuabudiwa kwa haki isipo kuwa Yeye. Basi mfanye Yeye tu ndiye wa kukutosha katika mambo yako yote, ndiye wa kutegemewa peke yake kama alivyo ahidi.

10 Na vumilia upuuzi wanao usema, na jitenge nao kwa moyo wako, na nenda kinyume na vitendo vyao, pamoja na kuwapuuzi, na kuacha kujilipizia.

11 Niachilie Mimi hao wanao kadhibisha, wenye kuneemeshwa, na uwape muhula muda mfupi.

12 Huko Akhera tumewawekea wanao kadhibisha pingu nzito, na Moto wa kuunguza, na chakula kinacho sakama kooni, hakimezeki, na adhabu yenye uchungu mkali usio stahamilika.

13 Tazama tanbihi ya 12.

14 Siku itakapo tikisika ardhi na milima kwa mtikiso mkubwa mno, na milima ikawa mirundu ya mchanga ulio tapanyika, baada ya kuwa mawe magumu yaliyo shikamana.

15 Enyi watu wa Makka! Hakika Sisi tumekutumieni Muhammad kuwa ni Mtume wa kukushuhudilieni Siku ya Kiyama kwa kukubali na kukataa, kama tulivyo mtuma Musa kwa Firauni awe ni Mtume. Firauni akamkataa huyo Mtume, basi tukamshika kwa mshiko wa nguvu!

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Basi mkikufuru mtajikinga vipi na adhabu ya Siku ambayo kwa kitisho chake itawafanya vijana wawe vikongwe wasio na nguvu?

18 Mbingu juu ya nguvu zake na ukubwa wake, Siku hiyo zitapasukilia mbali kwa shida zake na vitisho vyake. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni lazima itokee, hapana hivi wala hivi.

19 Hakika Aya hizi zinazo taja ahadi ya Mwenyezi Mungu ni mawaidha. Kwa hivyo mwenye kutaka kunafiika kwazo ataishika njia ya kumwendea Mola wake Mlezi kwa kuchamngu na kunyenyekea.

mnayo itanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtaikuta kwa Mwenyezi Mungu, imekuwa bora zaidi, na ina thawabu kubwa sana. Na mtakeni msamaha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.²⁰

20 Hakika Mola wako Mlezi anajua kwamba wewe, Muhammad, unakesha pengine akali kuliko thuluthi mbili za usiku, na mara nyengine unakesha nusu ya usiku, na pia wanakesha baadhi ya masahaba zako kama ukeshavyo wewe. Na hapana anaye weza kuukadiria urefu wa usiku na mchana, na kudhibiti saa zake, ila Mwenyezi Mungu. Yeye anajua kuwa hamwezi kuhisabu baraabara kila sehemu katika sehemu za usiku na mchana. Kwa hivyo amekukhafifishieni. Basi someni katika Sala kilicho chepesi katika Qur'ani. Yeye anajua kuwa watakuwepo kati yenu walio wagonjwa, ambao watapata taabu kukesha usiku; na wengine wamo safarini kwa ajili ya biashara na kazi, wakitafuta riziki ya Mwenyezi Mungu. Na wengine wanapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kulitukua Neno lake. Basi someni kilicho chepesi katika Qur'ani, na zishikeni baraabara faridha za Sala, na toeni Zaka iliyo kuwajibikieni, na mkopesheni Mwenyezi Mungu mkopo mwema, kwa kuwapa mafakiri kwa khiari juu ya hayo yaliyo kulazimuni. Na chochote cha kheri mnacho kitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu, mtakuta thawabu zake kwa Mwenyezi Mungu zimekuwa bora zaidi kuliko hicho mlichu kiacha na kukitoa, na malipo mema zaidi. Na mtakeni msamaha Mwenyezi Mungu kwa vitendo viovu na kwa upungufu katika vitendo vyema. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe madhambi ya Waumini, na ni Mwenye kuwarehemu.

Sura 74 - Al-Muddaththir

Utangulizi

Sura hii tukufu inamhimiza Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. awaonye watu wake, na amtukuze Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ayaache yasiyo faa kutokana naye, na imesimulia khabari za kupulizwa barugumu na shida za adhabu zitazo washukia makafiri. Na inamuamrisha Mtume s.a.w. amwachilie mbali anaye pinga fadhila alizo fanyiwa na kisha anatumai bado azidishiwe bila ya kutambua wala shukrani. Na Sura imebainisha vipi kulikuwa kufikiri kwa huyo mwenye kupinga na kuikataa Qur'ani, na ikafafanua vipi itakuwa adhabu yake katika Moto wa Saqar ambao unaelezwa kwa njia ya kutisha na kukhofisha. Na ikataja khabari za nafsi kwa zinavyo chuma kheri au shari, na ikaeleza hali ya watu wa mkono wa kulia na wanavyo wakejeli wakosefu kwa kuwauliza nini kilicho wasukumiza Motoni. Na Sura imekhitimisha kwa kusimulia kuwa Qur'ani ni ya mwenye kutaka kuwaidhika, na wenye kuwaidhika ndio watu wachamngu na ndio wenye kupata msamaha.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ewe uliye jigubika!¹
2. Simama uonye!²
3. Na Mola wako Mlezi mtukuze!³
4. Na nguo zako, zisafishe.⁴
5. Na yaliyo machafu yahame!⁵
6. Wala usitoe kwa kutaraji kuzidishiwa.⁶
7. Na kwa ajili ya Mola wako Mlezi, subiri!⁷
8. Basi litapo pulizwa barugumu,⁸
9. Siku hiyo, basi, itakuwa siku ngumu.⁹
10. Kwa makafiri haitakuwa nyepesi.¹⁰
11. Nische peke yangu na niliye muumba!¹¹

1 Ewe uliye jigubika kwa maguo! Inuka hapo kitandani, na uwahadharishe watu na adhabu ya Mwenyezi Mungu, ikiwa hawaamini. Na mkusudie Mola wako Mlezi makhsusi kwa kumtukuzwa. Na safisha nguo zako kwa maji kuzitoea najisi.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Tazama tanbihi ya 1.

5 Na iache adhabu, yaani kuwa daima mwenye kujitenga na yanayo pelekea kupata adhabu. Wala usimpe mtu yeyote kwa kutumai kupata zaidi kwake katika kile unacho mpa; na kwa ajili ya kumridhi Mola wako Mlezi subiri na stahamili juu ya maamrisha na makatazo, na kila jambo la juhudi na mashaka.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Tazama tanbihi ya 5.

8 Na litakapo pulizwa barugumu, huo ndio wakati wa siku ya shida kwa makafiri, wala si wepesi kwao kujitoea na majadiliano ya hisabu, na vitisho vyenginevyo.

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Tazama tanbihi ya 8.

11 Nische peke yangu na huyo niliye muumba. Kwani hakika Mimi ninatosha kukukifia mambo yake.

12. Na nikamjaalia awe na mali mengi,¹²
13. Na wana wanao onekana,¹³
14. Na nikamtengenezea mambo vizuri kabisa.¹⁴
15. Kisha anatumai nimzidishie!¹⁵
16. Hasha! Kwani hakika yeye alikuwa akizifanyia inadi Aya zetu!¹⁶
17. Nitamtesa kwa mateso yasio wezekana.¹⁷
18. Kwani hakika yeye alifikiri na akapima.¹⁸
19. Basi ameamgamia! Vipi alivyo pima!¹⁹
20. Tena ameamgamia! Vipi alivyo pima!²⁰
21. Kisha akatazama,²¹
22. Kisha akakunja kipaji, na akanuna.²²
23. Kisha akaipa kisogo haki, na akatakabari.²³
24. Na akasema: Haya si chochote ila ni uchawi ulio nukuliwa.²⁴
25. Haya si chochote ila kauli ya binaadamu.²⁵
26. Nitakuja mtia kwenye Moto wa Saqar.²⁶
27. Na nini kitakujuulisha ni nini huo Moto wa Saqar?²⁷
28. Haubakishi wala hausazi.²⁸
29. Unababua ngozi iwe nyeusi.²⁹
30. Juu yake wapo kumi na tisa.³⁰

Nimemjaalia mali yaliyo kunjuliwa yaliyo enea, yasio tindikia, na wana wanao tokea hadharani naye, na nikamkunjulia cheo na ukubwa kwa ukunjufu ulio timia. Kisha tena anatumai nimzidishie mali na wana na cheo bila ya shukrani yoyote!

12 Tazama tanbihi ya 11.

13 Tazama tanbihi ya 11.

14 Tazama tanbihi ya 11.

15 Tazama tanbihi ya 11.

16 Kuivunja hiyo tamaa yake, tunasema kwamba kwa kuwa yeye alikuwa akiikaadhibisha Qur'ani kwa inda, tutamgubika kwa adhabu yenye mashaka, wala hataweza kuikwepa.

17 Tazama tanbihi ya 16.

18 Hakika yeye amejifikiria nafsi yake, na akajitengenezea ya kuyasema ya kuitia ila Qur'ani, basi kwa hivyo amestahiki kuangamia huko. Vipi alivyo jilandalia kutia ila hiyo! Kisha akastahiki maangamizo hayo. Vipi alivyo jilandalia kutia ila hiyo.

19 Tazama tanbihi ya 18.

20 Tazama tanbihi ya 18.

21 Kisha akaziangalia nyuso za watu. Kisha akakunja uso wake, na akazidi kuukunja, kisha akaipa mgongo haki na akajivuna kuwa ati haitambui, na akasema: Haya si chochote ila ni uchawi ulio nukuliwa kutokana na watu wa kale.

22 Tazama tanbihi ya 21.

23 Tazama tanbihi ya 21.

24 Tazama tanbihi ya 21.

25 Maneno haya si chochote ila ni maneno ya viumbe aliy jifundisha Muhammad, na akadai kuwa ati yametoka kwa Mwenyezi Mungu.

26 Nitamtia Motoni aungue humo. Na nini kitakujuvya hiyo Jahannamu ni nini? Haibakishi nyama wala haisazi fupa ila italiunguza tu, ngozi ibabuke iwe nyeusi. Juu yake wako kumi na tisa wanao angalia kazi yake, na kuwaadhibu waliomo.

27 Tazama tanbihi ya 26.

28 Tazama tanbihi ya 26.

29 Tazama tanbihi ya 26.

30 Tazama tanbihi ya 26.

31. Na hatukuwafanya walinzi wa Motoni ila ni Malaika, wala hatukuifanya idadi yao hiyo ila kuwatatanisha walio kufuru, wapate kuwa na yakini walio pewa Kitabu, na wazidi Imani wale walio amini, wala wasiwe na shaka walio pewa Kitabu na Waumini, na wapate kusema wenye maradhi katika nyoyo zao na makafiri: Mwenyezi Mungu amekusudia nini kwa mfano huu? Ndio kama hivyo Mwenyezi Mungu humwacha apotee amtakaye, na humwongoa amtakaye. Na hapana yeyote anaye jua majeshi ya Mola wako Mlezi ila Yeye tu. Na haya si chochote ila ni ukumbusho kwa binaadamu.³¹
32. Hasha! Naapa kwa mwezi!³²
33. Na kwa usiku unapo kucha!³³
34. Na kwa asubuhi inapo pambazuka!³⁴
35. Hakika huo Moto ni katika mambo yaliyo makubwa kabisa!³⁵
36. Ni onyo kwa binaadamu,³⁶
37. Kwa anaye taka miongoni mwenu kutangulia au kuchelewa.³⁷
38. Kila nafsi imo rahanini kwa mabaya iliyo yachuma.³⁸
39. Isipo kuwa watu wa kuliani.³⁹
40. Hao watakuwa katika Mabustani, wawe wanaulizana⁴⁰
41. Khabari za wakosefu.⁴¹
42. Ni nini kilicho kupelekeni Motoni?⁴²
43. Waseme: Hatukuwa miongoni walio kuwa wakisali.⁴³

31 Na hatukuwafanya walinzi wa Motoni ila ni Malaika, na wala hatukuifanya idadi yao ya kumi na tisa ila kuwapa mtihani walio kufuru wapate yakini walio pewa Kitabu (yaani Biblia, Mayahudi na Wakristo) kwamba inayo sema Qur'ani juu ya walinzi wa Motoni ni kweli tupu itokayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kuwa hayo yanakubaliana na vinavyo sema vitabu vyao; na ili walio muamini Muhammad ipate kuzidi Imani yao. Na wala wasiyatilie shaka hayo walio pewa Kitabu na Waumini. Na wenye maradhi ya unaafiki katika nyoyo zao na makafiri waseme: Mwenyezi Mungu anataka nini kwa idadi hii ya ajabu? Kwa mfano kama huu ulio tajwa, wa kupoteza na kuongoa, ndio Mwenyezi Mungu huwapoteza makafiri na huwaongoa Waumini. Na hapana anaye wajua askari wa Mola wako Mlezi, jinsi walivyo kuwa wengi mno, ila Yeye *Subhanahu* wa Taala. Na huo Moto si chochote ila ni kumbusho na kitisho kwa binaadamu.

32 Kuzidi kumhadharisha anaye onywa naye asiogope, ninaapa kwa mwezi na usiku unapo ondoka, na kwa asubuhi inapo angaza na kuchomoza, kwamba huo Moto ni moja katika vitisho vikubwa kabisa yva kuonya na kukhofisha.

33 Tazama tanbihi ya 32.

34 Tazama tanbihi ya 32.

35 Tazama tanbihi ya 32.

36 Tazama tanbihi ya 32.

37 Ni onyo kwa binaadamu kwa atakaye kuja mbele katika nyinyi kutenda kheri, au kubaki nyuma asitende.

38 Kila nafsi itashikwa kwa iliyo yatenda, ila Waislamu walio zigombo shingo zao kwa ut'iifu.

39 Tazama tanbihi ya 38.

40 Hao watakuwa katika Mabustani ya Peponi, ambayo hayaweze kani kusifika. Wataulizana wao kwa wao khabari za wakosefu, wakiuliza hali zao nini kilicho watia Motoni?

41 Tazama tanbihi ya 40.

42 Tazama tanbihi ya 40.

43 Waseme: Hatukuwa miongoni mwa wenye kusali kama wasalivyo Waislamu. Wala hatukuwa tukiwalisha masikini kama Waislamu walivyo kuwa wakilisha. Na tulikuwa tukijisoza na kuzama katika upotovu na mazungumzo ya uwongo pamoja na hao walio kuwa wakiporojoka. Na tulikuwa tukiikadhibisha Siku ya Hisabu, mpaka ikatujia yakini, yaani maut.

44. Wala hatukuwa tukiwalisha masikini.⁴⁴
45. Na tulikuwa tukizama pamoja na walio zama katika maovu.⁴⁵
46. Na tulikuwa tukiikanusha siku ya malipo.⁴⁶
47. Mpaka yakini ilipo tufikia.⁴⁷
48. Basi hautawafaa kitu uombezi wa waombezi.⁴⁸
49. Basi wana nini hata wanapuuza onyo hili?⁴⁹
50. Kama kwamba wao ni mapunda walio timuliwa,⁵⁰
51. Wanao mkimbia simba!⁵¹
52. Ati kila mmoja katika wao anataka apewe nyaraka zilizo funuliwa.⁵²
53. Hasha! Kwani wao hawaiogopi Akhera?⁵³
54. Hasha! Kwa hakika huu ni ukumbusho!⁵⁴
55. Basi anaye taka atakumbuka.⁵⁵
56. Na hawatakumbuka isipo kuwa Mwenyezi Mungu atake. Uchamngu ni kwake Yeye, na msamaha ni wake Yeye.⁵⁶

44 Tazama tanbihi ya 43.

45 Tazama tanbihi ya 43.

46 Tazama tanbihi ya 43.

47 Tazama tanbihi ya 43.

48 Basi hao hakuto waokoa kuombewa msamaha na waombezi, wakiwa ni Malaika, au Manabii, au watu wema.

49 Basi wana nini hata wanajitenga na mawaidha ya Qur'ani?

50 Hao hakika wamekuwa kama punda wanao toka mbio kumkimbia anaye wafukuza.

51 Tazama tanbihi ya 50.

52 Bali kila mmoja wao anataka apewe ukurasa unao toka mbinguni uwazi ulio funguliwa unao thibitisha ukweli wa Mtume s.a.w. (yaani kama shahada ya Ujumbe wake kwao!)

53 Juu ya kuzidi kuwaonya kwa hayo wayatakayo bali hawaikhofu Akhera, na wakapuuza mawaidha, na wakavumbua mbinu mbali mbali za kutaka miujiza na Ishara.

54 Ni hakika isiyo na shaka kuwa Qur'ani ni mawaidha na ukumbusho wa kutosha kufikisha Ujumbe. Mwenye kutaka kukumbuka wala asisahau basi na atende.

55 Tazama tanbihi ya 54.

56 Na wala hawatakumbuka ila Mwenyezi Mungu atake Mwenyewe, kwani Yeye ndiye anaye stahiki kuogopwa, na Yeye ndiye wa kumsamehe mwenye kumcha.

Sura 75 - Al-Qiyamah

Utangulizi

Sura hii tukufu inasimulia khabari za kufufuliwa watu na kuhisabiwa, na khabari za Kiyama na vitisho vyake. Kisha inampa moyo Mtume s.a.w. kuwa Qur'ani itakusanywa yote katika kifua chake, na Sura ikageuka kuwakemea hao wanao penda yapitayo njia ya duniani, wakaacha ya Akhera, na ikalinganisha baina ya nyuso za Waumini zenye kung'aa na nyuso za makafiri zilizo kunjana. Na imezungumzia pia hali ya mtu aliye mguu mmoja uko kaburini, na aliyo nayo ya upungufu katika yaliyo kuwa yakimlazimu, hata akawa kama kwamba anadhani kuwa hatahisabiwa yeye. Na mwisho Sura imekhitimisha kwa dalili zinazo pelekea lazima tuamini kuwa kufufuliwa kupo

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ninaapa kwa Siku ya Kiyama!¹
2. Na ninaapa kwa nafsi inayo jilaumu!²
3. Anadhani mtu kuwa Sisi hatutaikusanya mifupa yake?³
4. Kwani! Sisi tunaweza hata kuziweka sawa sawa ncha za vidole vyake!⁴
5. Lakini mtu anataka tu kuendelea na maasi kwa siku zilioko mbele yake.⁵
6. Anauliza: Lini itakuwa hiyo Siku ya Kiyama?⁶
7. Basi jicho litapo dawaa,⁷
8. Na mwezi utapo patwa,⁸
9. Na likakusanywa jua na mwezi,⁹
10. Siku hiyo mtu atasema: Yako wapi makimbilio?¹⁰
11. La! Hapana pa kukimbilia!¹¹

1 Ninaapa na natilia mkazo kiapo hichi kwa Siku ya Kiyama, na hiyo ni kweli iliyo thibiti; na ninaapa na natilia mkazo kiapo hichi kwa nafsi inayo mlaumu mtu kwa dhambi zake na upungufu wake, ya kwamba bila ya shaka yoyote mtafufuliwa baada ya kukusanywa mafupa yenu yaliyo tawanyika. Hivyo mtu anadhani baada ya kuwa Sisi tulimumba naye hakuwa kitu chochote, tutakuja shindwa kuyakusanya mafupa yake yaliyooza na yakatapanika?

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Hasha! Sisi tuna uweza wa kuviweka sawa hata vifupa vya vidole vyake vilivyo vurugika, wachilia mbali mafupa yake makubwa makubwa ya mwili wake.

5 Hivyo mtu anakanya kufufuliwa? Anataka abakie katika uasi wake katika siku zote zilizo mbakilia katika umri wake ulio salia?

6 Anauliza kwa kuona haiwezi kutokea saa ya Kiyama: Lini itakuwa hiyo Siku ya Kiyama?

7 Jicho litapo tahayari kwa kufazaika na kushtuka, na mwangaza wa mwezi ukapotea, na jua likakusanyika na mwezi kuchomoza magharibi, mtu hapo atasema: Yako wapi makimbilio kuikimbia hii adhabu?

8 Tazama tanbihi ya 7.

9 Tazama tanbihi ya 7.

10 Tazama tanbihi ya 7.

11 Huachi, ewe mtu, kutafuta makimbilio? Leo huna pa kukimbilia wewe, ila kwa Mola wako Mlezi peke yake, ndipo penye matulivu ya waja, Peponi au Motoni.

12. Siku hiyo pa kutua ni kwa Mola wako Mlezi tu.¹²
13. Siku hiyo ataambiwa aliyo yatanguliza na aliyo yaakhirisha.¹³
14. Bali mtu ni hoja juu ya nafsi yake.¹⁴
15. Na ingawa atatoa chungu ya udhuru.¹⁵
16. Usiutikisie huu wahyi ulimi wako kwa kuufanyia haraka.¹⁶
17. Hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha.¹⁷
18. Tunapo usoma, basi nawe fuatiliza kusoma kwake.¹⁸
19. Kisha ni juu yetu kuubainisha.¹⁹
20. Hasha! Bali nyinyi mnapenda maisha ya duniani,²⁰
21. Na mnaacha maisha ya Akhera.²¹
22. Zipo nyuso siku hiyo zitao ng'ara,²²
23. Zinamwangalia Mola wao Mlezi.²³
24. Na zipo nyuso siku hiyo zitakao kunjana.²⁴
25. Zitajua ya kuwa zitafikiwa na livunjalo uti wa mgongo.²⁵
26. La, hasha! (Roho) itakapo fikia kwenye mafupa ya koo,²⁶
27. Na pakasemwa: Nani wa kumganga?²⁷
28. Na mwenyewe akajua kwa hakika kuwa huko ndiko kufariki;²⁸
29. Na utapo ambatishwa muundi kwa muundi,²⁹
30. Siku hiyo ndiyo kuchungwa kupelekwa kwa Mola wako Mlezi!³⁰

12 Tazama tanbihi ya 11.

13 Siku hiyo mtu ataambiwa vitendo vyake alivyo vitanguliza na alivyo viakhirisha.

14 Bali mtu yeye mwenyewe ni hoja iliyo wazi juu ya nafsi yake inayo mkazania kwa anayo yatenda na anayo yaacha. Na ijapo kuwa atajitolea chungu nzima ya udhuru na akazieneza, hawezi kabisa kuepukana na hoja hizo.

15 Tazama tanbihi ya 14.

16 Usiuharikishe ulimi wako kwa kuisoma Qur'ani na kujaribu kuihifadhi kwa haraka pale unapo teremshiwa kwa Wahyi. Hakika ni juu yetu Sisi kuikusanya hiyo katika kifua chako, na kuithibitisha katika ulimi wako.

17 Tazama tanbihi ya 16.

18 Akikusomea Mjumbe wetu (Jibril) basi nawe ifuatilize kama unavyo isikia. Kisha baada ya hayo ni juu yetu kuibainisha ikiingia tatizo lolote juu yako.

19 Tazama tanbihi ya 18.

20 Wacheni kukanya kufufuliwa, na hilo ni jambo la kweli. Lakini nyinyi mnaipenda dunia na starehe zake, na mnaicha Akhera na neema zake.

21 Tazama tanbihi ya 20.

22 Siku hiyo zitakuwapo nyuso nzuri, zenye kumwangalia Mola wao Mlezi bila ya kusema kwa sifa gani, wajiji gani, au masafa gani. (Tazama Maelezo 75:22)

23 Tazama tanbihi ya 22.

24 Na nyuso nyengine zitakuwapo zimenuna, zimekunjana mno, zinangojea zitendewe jambo ambalo kwa kitisho chake linavunja uti wa mgongo.

25 Tazama tanbihi ya 24.

26 Mna nini na kuipenda dunia ambayo mnaifariki roho inapo fika katika mafupa ya kooni, na walio hudhuria wakasema: Yupo wa kumganga huyu kwa haya aliyo nayo? Akayakinisha yule yaliyo mfika mauti kama lililo mshukia ni kuiacha dunia inayo pendwa, na imekwisha mfika shida yake kikomo cha mwisho. Na muundi wa mguu umekwisha ambatana na wa pili wakati wa kutoka roho. Kwa Mola wako Mlezi tu siku hiyo ndio machungio ya waja, ama Peponi au Motoni.

27 Tazama tanbihi ya 26.

28 Tazama tanbihi ya 26.

29 Tazama tanbihi ya 26.

30 Tazama tanbihi ya 26.

31. Kwa sababu hakusadiki, wala hakusali.³¹
32. Bali alikanusha, na akageuka.³²
33. Kisha akenda kwa ahali zake kwa matao.³³
34. Ole wako, ole wako!³⁴
35. Kisha Ole wako, ole wako!³⁵
36. Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure?³⁶
37. Kwani hakuwa yeye tone ya manii lilio shushwa?³⁷
38. Kisha akawa kidonge cha damu, tena Mwenyezi Mungu akamuumba na akamtengeneza vilivyo.³⁸
39. Kisha akamfanya namna mbili, mwanamume na mwanamke.³⁹
40. Je! Huyu hakuwa ni Muweza wa kufufua wafu?⁴⁰

31 Binaadamu amekanya kufufuliwa, na kwa hivyo hakumsadiki Mtume wala Qur'ani. Wala hakumtimizia Mwenyezi Mungu faridha za Sala. Lakini alihakadhibisha Qur'ani, akaipuuza Imani, na akatoka kwenda kwa watu wake wa nyumbani kwa maringo na kujitapa.

32 Tazama tanbihi ya 31.

33 Tazama tanbihi ya 31.

34 Ewe unaye kadhibisha, utaangamia! Tena utaangamia! Na tena utaangamia, na utaangamia!

35 Tazama tanbihi ya 34.

36 Hivyo anadhani huyu mtu anaye kanya kufufuliwa kuwa ataachwa hivi hivi akiringa tu katika maisha yake, na akisha kufa iwe basi, wala asifufuliwe akahisabiwa kwa vitendo vyake?

37 Kwani yeye mtu hakuwa ni tone tu ya manii, ilio jaaliwa kuwemo katika tumbo la uzazi? Kisha hiyo tone ikawa kipande cha damu iliyo ganda, na Mwenyezi Mungu akaiumba, akaisawazisha mpaka ikawa na umbo zuri?

38 Tazama tanbihi ya 37.

39 Akajaalia namna mbili, mwanamume na mwanamke?

40 Je! Huyu Muumba wa mwanzo aliye fanya yote haya, basi si muweza wa kuwahuisha maiti baada ya kuyakusanya mafupa yao?

Sura 76 - Al-Insan

Utangulizi

Sura hii imekusanya maneno juu ya kuumbwa kwa binaadamu na kujaribiwa kwake, na kutayarishwa kwake aweze kumshukuru Mwenyezi Mungu au kumkufuru. Na imekusanya mazungumzo juu ya malipo ya makafiri; na imefafanua neema alizo wafadhili Mwenyezi Mungu Waumini, kisha ikageukia kusema na Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. na kumtaja alivyo neemeshwa kwa kuteremshiwa Qur'ani, na ikamuamrisha asubiri na adumu katika ut'iifu. Na Sura inawaonya wanao ipenda dunia wakaifadhilisha kuliko Akhera, na ikasimulia kwa mawaidha ya Aya hizi, na ikakhusisha kunafiika kwazo pindi akipenda Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ikazifanya rehema za Mwenyezi Mungu na adhabu zake kuwa zinategemea hukumu yake na pendo lake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Hakika kilimpitia binaadamu kipindi katika zama ambacho kwamba hakuwa kitu kinacho tajwa.¹
2. Hakika Sisi tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyo changanyika, tumfanyie mtihani. Kwa hivyo tukamfanya mwenye kusikia, mwenye kuona.²
3. Hakika Sisi tumembainishia Njia. Ama ni mwenye kushukuru, au mwenye kukufuru.³
4. Hakika Sisi tumewaandalia makafiri minyororo na pingu na Moto mkali.⁴
5. Hakika watu wema watakunywa katika vinywaji vilivyo changanyika na kafuri,⁵
6. Ni chemchem watakao inywa waja wa Mwenyezi Mungu, wakiifanya imiminike kwa wingi.⁶
7. Wanatimiza ahadi, na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana,⁷
8. Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa.⁸
9. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihwa wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani.⁹

1 Hakika kimempitia mwanaadamu kipindi cha zama kabla hajapuliziwa roho, naye hata bado hakuwa ni kitu cha kutajika kwa jina lake, wala hajuulikani nini atakuwa.

2 Hakika Sisi tumemuumba mwanaadamu naye ana sifa namna mbali mbali, kwa ajili ya kumtia mtihanini, majaribioni, baadaye. Kwa hivyo tukamjaalia awe anasikia na anaona, ili apate kuzisikia Aya na azione Ishara.

3 Hakika Sisi tumembainishia Njia ya Uwongofu, ama awe Muumini au awe kafiri.

4 Hakika Sisi tumewawekea tayari makafiri minyororo kuwafungia miguu yao, pingu za kuwafungia mikono na shingo, na moto unao waka.

5 Hakika walio kuwa wakweli katika Imani yao watakunywa mvinyo iliyo changanywa na maji ya kafuri. Hiyo ni chemchem wanayo inywa waja wa Mwenyezi Mungu, na wanaipitisha watakapo kwa sahala.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Wanatekeleza yaliyo wajibikia, na wanaikhofu Siku kubwa hiyo ambayo madhara yake yataenea kote kote.

8 Na huwalisha chakula mafakiri wasio weza kazi, na watoto walio fiwa na wazee wao, na wafungwa wasio miliki kitu, ijapo kuwa wao wenyewe hao watoaji wanakipenda hicho wanacho kitoa, na wanakihitajia.

9 Na hujiambia nafsi zao: Hakika sisi tunakulisheni kwa ajili ya kutaka thawabu za Mwenyezi Mungu.

10. Hakika sisi tunaogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu.¹⁰
11. Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha.¹¹
12. Na atawajazi Bustani za Peponi na maguo ya hariri kwa vile walivyo subiri.¹²
13. Humo wataegemea juu ya viti vya enzi, hawataona humo jua kali wala baridi kali.¹³
14. Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao, na mashada ya matunda yataning'inia mpaka chini.¹⁴
15. Na watapitishiwa vyombo vya fedha na vikombe vya vigae,¹⁵
16. Vya fedha safi kama kiyoo, wamevipima kwa vipimo.¹⁶
17. Na humo watanyeshwa kinywaji kilicho changanyika na tangawizi.¹⁷
18. Hiyo ni chemchem iliyo humo inaitwa Salsabil.¹⁸
19. Na watawazungukia kuwatumikia wavulana wasio pevuka, ukiwaona utawafikiri ni lulu zilizo tawanywa.¹⁹
20. Na utakapo yaona, utakuwa umeona neema na ufalme mkubwa.²⁰
21. Juu yao zipo nguo za hariri laini za kijani kibichi, na hariri nzito ya at'ilasi. Na watavikwa vikuku vya fedha, na Mola wao Mlezi atawanyweshwa kinywaji safi kabisa.²¹
22. Hakika haya ni malipo yenu; na juhudi zenu zimekubaliwa.²²
23. Hakika Sisi tumekuteremshia Qur'ani kidogo kidogo.²³
24. Basi ngojea hukumu ya Mola wako Mlezi wala usimt'ii miongoni mwao mwenye dhambi au mwenye kufuru.²⁴

Sisi hatutaki kwenu malipo au zawadi, wala hatutaki kushukuriwa na kusifiwa.

10 Hakika sisi tunakhofu kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku ya kumletea msiba atakaye kuwapo siku hiyo, na siku ya watu kukunja nyuso zao na vipaji vyao.

11 Basi Mwenyezi Mungu akawalinda na shida za siku hiyo, na badala ya mkunjo wa wenye maasi, akawapa nyuso za kupendeza, na ukunjufu na furaha katika nyoyo zao, na akawajazi kwa ile subira yao Pepo imeenea furaha, na nguo zake ni hariri laini.

12 Tazama tanbihi ya 11.

13 Wakiegemea huko Peponi juu ya makochi, hawaoni joto la jua, wala shida ya baridi.

14 Na Pepo ambayo vivuli vya miti yake vimeenea kote kote, na matunda yake mepesi kuyachuma.

15 Na wakiwazungukia watumishi wao kwa bilauri za kunywa zilio fanywa kwa fedha, lakini unaona kiliomo ndani kama kwamba ni kigae, na vinapimwa vinywaji kwa kadiri wanavyo penda wanywaji.

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Na watu wema hupewa kunywa huko Peponi mvinyo inayo fanana na sharubati ya tangawizi kwa utamu. Hiyo ni kutokana na chemchem ya Peponi inayo itwa Salsabil, kwa sababu ya wepesi wa unywaji wake na uzuri wake.

18 Tazama tanbihi ya 17.

19 Na watakuwa wanawazunguka vijana ambao hawabadiliki hali yao, kwa furaha na sururi. Ukiwaona wanapo zunguka kwa wepesi na uchangamfu, utawadhania kwa uzuri wao na usafi wa rangi zao, kama lulu zilizo tandazwa mbele yako zinang'ara.

20 Na ukitazama popote katika hiyo Pepo utaona neema kubwa, na ufalme ulio tanda.

21 Juu yao zipo nguo za hariri nyepesi za kijani, na nguo za hariri nzito. Na mapambo yao yaliomo mikononi mwao ni vikuku vya fedha. Na Mola wao Mlezi atawanyweshwa kinywaji kingine kilio safi, hakina uchafu wala najisi.

22 Hakika neema hizi ameziandaa kwa kukulipeni kwa vitendo vyenu. Na hizo juhudi zenu duniani ni zenye kusifika kwa Mwenyezi Mungu, na zinampendeza, na zimekubaliwa.

23 Hakika Sisi, kwa rehema yetu na hikima yetu, tumekuteremshia wewe Qur'ani kwa njia ya kukutuzia moyo wako, na uweze daima kuihifadhi, basi huto isahau kabisa.

24 Basi subiri, uivumilie hikima ya Mola wako Mlezi kwa kuakhirisha kushinda kwako kuwashinda maadui zako, na wewe ukapata mithani kwa maudhi yao. Wala usiwat'ii washirikina, wingi wa madhambi, walio zama katika ukafiri.

- 25.** Na likumbuke jina la Mola wako Mlezi asubuhi na jioni;²⁵
26. Na usiku msjudie Yeye, na umtakase usiku, wakati mrefu.²⁶
27. Kwa hakika watu hawa wanapenda maisha ya kidunia, na wanaiacha nyuma yao siku nzito.²⁷
28. Sisi tumewaumba, na tukavitia nguvu viungo vyao. Na tukitaka tutawabadilisha mfano wao wawe badala yao.²⁸
29. Hakika haya ni mawaidha; basi anaye taka atashika Njia ya kwenda kwa Mola wake Mlezi.²⁹
30. Wala hamwezi kutaka ila atakapo Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye ilimu, Mwenye hikima.³⁰
31. Humuingiza amtakaye katika rehema yake. Na wenye kudhulumu amewawekea adhabu iliyo chungu.³¹

25 Na dumisha kumkumbuka na kumtaja Mola wako Mlezi, na sali alfajiri mapema, na adhuhuri, na alasiri jioni, na usiku sali magharibi na isha. Na fanya ibada za usiku kwa muda mrefu.

26 Tazama tanbihi ya 25.

27 Hakika hawa makafiri wanaipenda dunia, na wanaifadhilisha kuliko Akhera. Na wanaiacha migongoni mwao siku yenye misiba mikubwa, na vitisho vikali. Wala wao hawajui nini cha kuwaokoa wao na hayo!

28 Sisi tumewaumba wao, na tumefanya kwa hikima kuumbwa kwao. Na tukitaka tutawateketeza wao na tutawaleta mfano ya wao badala yao, ambao hao watakuja kumt'ii Mwenyezi Mungu kinyume na wao.

29 Hakika Sura hii ni mawaidha kwa walimwengu wote. Basi mwenye kutaka atafuata njia ya Imani na uchamngu kwendea kwa Mola wake Mlezi imfikishe kwenye maghfira yake na Pepo yake.

30 Wala nyinyi hamwezi kutaka kitu chochote ila wakati anapo taka Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuzijua hali zenu, Mwenye hikima kwa anayo yataka na akayakhiari.

31 Humuingiza amtakaye katika Pepo yake. Basi kuingia Peponi ni kwa fadhila na rehema ya Mwenyezi Mungu. Naye amewadhalilisha wenye kudhulumu, amewatengenezea adhabu iliyo chungu.

Sura 77 - Al-Mursalaat

Utangulizi

Lilio muhimu kabisa katika yaliyo kusanywa na Sura hii tukufu ni maneno yaliyo khusu kufufuliwa, na Kiyama, na dalili za kuthibitisha kuwa kitatokea, na kutishwa kwa waliyo yakataa hayo, na kurudishwa kutishwa huko kwa “Ole wao” mara kumi, na kuwatisha kwa unyonge na adhabu itayo wapata; na kubashiriwa wachamngu kwa starehe na neema watazo zikuta, na mwisho wake masaiibu yatayo wapata makafiri wasio iamini Qur’ani.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa zinazo tumwa kwa upole!¹
2. Na zinazo vuma kwa kasi!²
3. Na zikaeneza maeneo yote!³
4. Na zinazo farikisha zikatawanya!⁴
5. Na zinazo peleka mawaidha!⁵
6. Kwa kuudhuru au kuonya,⁶
7. Hakika mnayo ahidiwa bila ya shaka yatakuwa!⁷
8. Wakati nyota zitakapo futwa,⁸
9. Na mbingu zitakapo pasuliwa,⁹
10. Na milima itakapo peperushwa,¹⁰
11. Na Mitume watakapo wekewa wakati wao,¹¹
12. Kwa siku gani hiyo wamewekewa muda huo?¹²

1 Naapa kwa Aya zilizo tumwa kwa ulimi wa Jibrili kumpelekea Muhammad kwa upole wa kawaida na kheri, na kwa Aya zenye kuzitwaa kwa nguvu dini nyengine zote za uwongo zikizipeperushia mbali, na kwa Aya zenye kueneza hikima na uwongofu katika nyoyo za walimwengu kwa uenezi mkubwa mno, na zenye kufarikisha baina ya kweli na uwongo kwa mfarakano ulio wazi kabisa, na zenye kuwapa watu mawaidha ya kuwanufaisha, ili iwe ni udhuru kwao na onyo wasiwe na hoja, hakika haya mliyo ahidiwa ya kuja Kiyama kwa yakini yatatimia tu bila ya shaka yoyote.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Tazama tanbihi ya 1.

5 Tazama tanbihi ya 1.

6 Tazama tanbihi ya 1.

7 Tazama tanbihi ya 1.

8 Basi nyota zitapo ondolewa kabisa, na mbingu zitapo pasuka, na milima ikavurugwa na ikapeperushiwa mbali na upepo, na Mitume wakawekewa wakati maalumu wahudhurie kwa ajili ya kuwatolea ushahidi kaumu zao.

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Tazama tanbihi ya 8.

11 Tazama tanbihi ya 8.

12 Kwa ajili ya siku gani yametayarishwa mambo haya makubwa makubwa? Kwa ajili ya siku watakapo pambanuliwa baina ya viumbe. Na nini cha kukujuvya ina nini hiyo siku ya kupambanua? Ni maangamio ya milele siku hiyo kwa hao wanao kadhibisha walio waahidi Mitume!

13. Kwa siku ya kupambanua!¹³
14. Na nini kitakacho kujuulisha siku ya kupambanua ni nini?¹⁴
15. Ole wao, siku hiyo hao wanao kanusha!¹⁵
16. Kwani hatukuwaangamiza walio tangulia?¹⁶
17. Kisha tukawafuatilizia walio fuatia?¹⁷
18. Ndio kama hivi tuwatendavyo wakosefu!¹⁸
19. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!¹⁹
20. Kwani hatukukuumbeni kwa maji ya kudharauliwa?²⁰
21. Kisha tukayaweka mahali pa utulivu madhubuti?²¹
22. Mpaka muda maalumu?²²
23. Tukakadiria na Sisi ni wabora wa kukadiria.²³
24. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!²⁴
25. Kwani hatukuifanya ardhi yenye kukusanya?²⁵
26. Walio hai na maiti?²⁶
27. Na ndani yake tukaweka milima mirefu yenye kuthibiti, na tunakunywesheni maji matamu?²⁷
28. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!²⁸
29. Nendeni kwenye adhabu mliyo kuwa mkiikanusha!²⁹
30. Nendeni kwenye kivuli chenye mapande matatu!³⁰
31. Hakikingi moto, wala hakiwaepushi na mwako.³¹

13 Tazama tanbihi ya 12.

14 Tazama tanbihi ya 12.

15 Tazama tanbihi ya 12.

16 Kwani hatukuwaangamiza mataifa ya zamani yaliyo kadhibisha, na kisha tukawafuatilizia hao wenginewe tukawateketeza hali kadhaalika, kwa madhambi waliyo yafanya na walivyo mkataa Mwenyezi Mungu?

17 Tazama tanbihi ya 16.

18 Tazama tanbihi ya 16.

19 Siku hiyo ni siku ya kuteketezwa walio kadhibisha, kama tulivyo waahidi.

20 Kwani hatukukuumbeni kutokana na maji yaliyo dhalili, nayo ni manii, na tukayaweka maji haya katika pahala patulivu, mpaka kutimilia kuumbwa kwake na kutengenezwa kwake kwa muda anao ujua Mwenyezi Mungu. Nasi tukaweka vipimo katika kuumbwa kwake, na kutengenezwa kwake, na kutoka kwake. Basi wabora wa kupima na kukadiria ni Sisi. Ole wao hao wanao kadhibisha neema za kuumba na kukadiria.

21 Tazama tanbihi ya 20.

22 Tazama tanbihi ya 20.

23 Tazama tanbihi ya 20.

24 Tazama tanbihi ya 20.

25 Kwani hatukuifanya ardhi kuwa imekusanya juu ya mgongo wake viumbe vilivyo hai visio hisabika, na vilio kufa visio kadirika, na tukaweka milima iliyo thibiti imara mirefu, na tukakunywesheni maji matamu? Wataangamia siku hiyo hao wanao kadhibisha neema hizi!

26 Tazama tanbihi ya 25.

27 Tazama tanbihi ya 25.

28 Tazama tanbih ya 25.

29 Siku ya kupambanua wataambiwa makafiri: Nendeni huko Motoni mliko kuwa mkikukanusha. Nendeni kwenye joto la moshi wa Jahannamu ulio gawika kwa ukubwa wake mapande matatu. Hapana cha kujikinga na joto la siku hiyo, wala kivuli hicho hakipunguzi joto la mwako hata kidogo.

30 Tazama tanbihi ya 29.

31 Tazama tanbihi ya 29.

32. Hakika Moto huo unatoa macheche kama majumba!³²
33. Kama kwamba ni ngamia wa rangi ya manjano!³³
34. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!³⁴
35. Hii ni siku ambayo hawatatamka kitu,³⁵
36. Wala hawataruhusiwa kutoa udhuru.³⁶
37. Ole wao siku hiyo hao walio kanusha!³⁷
38. Hii ndiyo siku ya kupambanua. Tumekukusanyeni nyinyi na walio tangulia.³⁸
39. Ikiwa mnayo hila, nifanyieni hila Mimi!³⁹
40. Ole wao siku hiyo hao walio kanusha!⁴⁰
41. Hakika wachamngu watakuwa katika vivuli na chemchem,⁴¹
42. Na matunda wanayo yapenda,⁴²
43. Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa yale mliyo kuwa mkiyatenda.⁴³
44. Hakika ndio kama hivyo tunavyo walipa watendao mema.⁴⁴
45. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!⁴⁵
46. Kuleni na mjifurahishe kidogo tu. Hakika nyinyi ni wakosefu!⁴⁶
47. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!⁴⁷
48. Na wakiambiwa: Inameni! Hawainami.⁴⁸

32 Moto huo hutupa macheche yenye ukubwa kama majumba, au utaona hayo macheche kama ngamia weusi wenye kuingia rangi ya manjano. Wataangamia siku hiyo wanao kanusha kwamba hizi ndizo sifa za Moto.

33 Tazama tanbihi ya 32.

34 Tazama tanbihi ya 32.

35 Haya uliyo simuliwa yataokea katika siku ambayo hawatatamka kitu cha kuwanufaisha, wala hawatakuwa na idhini ya kutamka, wala hawatatoa udhuru, kwani hawana udhuru. Wataangamia siku hiyo wanayo ikadhibisha siku hii.

36 Tazama tanbihi ya 35.

37 Tazama tanbihi ya 35.

38 Hii ndiyo siku ya kufafanua baina ya mwenye ukweli, na mwenye uwongo, kwa kuwa kila mmoja atalipwa kwa mujibu wa anavyo stahiki. Enyi mnao mkadhibisha Muhammad! Tumekujaalieni nyinyi na walio kutangulieni walio kadhibisha mfano wenu, kama mnayo hila ya kujikinga na adhabu basi fanyeni hila hiyo. Basi njooni muepukane na adhabu yangu. Wataangamia siku hiyo wanayo ikadhibisha ahadi ya Mwenyezi Mungu.

39 Tazama tanbihi ya 38.

40 Tazama tanbihi ya 38.

41 Hakika wachamngu wenye kujikinga na adhabu ya Mwenyezi Mungu watakuwa katika kivuli kikubwa, na chemchem zinazo miminika, na matunda wanayo yaonea ladha, na wanayo yapenda, wataambiwa kwa kuamkiwa na kukirimiwa: Kuleni na mnywe chakula na vinywaji kwa starehe kwa sababu ya vitendo vyema mlivyo kuwa mkivitenda duniani. Hakika Sisi huwalipa mfano wa malipo hayo matukufu watu wema. Wataangamia siku hiyo wanayo ikadhibisha Pepo.

42 Tazama tanbihi ya 41.

43 Tazama tanbihi ya 41.

44 Tazama tanbihi ya 41.

45 Tazama tanbihi ya 41.

46 Na makafiri wataambiwa: Kuleni na mjistareheshe kwa starehe isiyo baki muda mrefu, kwani hakika nyinyi ni wakosefu kwa kumshirikisha kwenu Mwenyezi Mungu. Wataangamia siku hiyo wanao ikadhibisha neema.

47 Tazama tanbihi ya 46.

48 Na wakiambiwa: Salini kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na mnyenyekeeni Yeye, hawanyenyekei wala hawasali; bali hushikilia kiburi chao! Wataangamia siku wanao kadhibisha amri za Mwenyezi Mungu na makatazo yake.

49. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!⁴⁹

50. Basi maneno gani baada ya haya watayaamini?⁵⁰

49 Tazama tanbihi ya 48.

50 Basi maneno gani hawa watayaamini ikiwa hawaiamini Qur'ani, na hali hii ni muujiza ulio toka mbinguni?

Sura 78 - An-Naba'

Utangulizi

Sura hii imethibitisha khabari ya kufufuliwa, na inawahadharisha hao wenye kutilia shaka jambo hilo. Na ikasimamisha hoja na dalili juu ya kuwezekana kwake kwa kuyaeleza yanayo onekana ya kudra ya Mwenyezi Mungu. Na ikatilia mkazo kuwepo kwake, na ikataja baadhi ya alama zake. Kisha ikataja khatima ya wenye kuasi, na khatima ya wachamngu. Na ikamalizikia kwa kuonya na kukhofisha kwa siku hiyo inayo tisha.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. WANAUUZANA nini?¹
2. Ile khabari kuu,²
3. Ambayo kwayo wanakhitalifiana.³
4. La! Karibu watakuja jua.⁴
5. Tena la! Karibu watakuja jua.⁵
6. Kwani hatukuifanya ardhi kama tandiko?⁶
7. Na milima kama vingi?⁷
8. Na tukakuumbeni kwa jozi?⁸
9. Na tukakufanya kulala kwenu ni mapumziko?⁹
10. Na tukaufanya usiku ni nguo?¹⁰
11. Na tukaufanya mchana ni wa kuchumia maisha?¹¹
12. Na tukajenga juu yenu saba zenye nguvu?¹²
13. Na tukaifanya taa yenye mwanga na joto,¹³
14. Na tukateremsha maji yanayo anguka kwa kasi kutoka mawinguni,¹⁴

1 Wanaulizana nini hao makafiri?

2 Wanaulizana khabari kubwa, khabari ya kufufuliwa, ambayo wao wamezama ndani yake kukhitalifiana baina ya wenye kuikataa na wenye kuitilia shaka.

3 Tazama tanbihi ya 2.

4 Kuwazuia kuulizana huko wanaambiwa kuwa watakuja ujua ukweli wa mambo hapo watapo ona kufufuliwa kumetokea khasa.

5 Tena kuwazuia, watakuja jua itapo wateremkia adhabu.

6 Kwani wao hawaoni Ishara za uweza wetu kwamba Sisi tumeifanya ardhi imetandikwa upatikane utulivu juu yake na iwezekane kutembea juu yake?

7 Na tukaifanya milima ni vingi vya ardhi vya kuituliza? (*Tazama Maelezo 78:7*)

8 Na tukakuumbeni kwa jozi, wanaume na wanawake.

9 Na tukafanya kulala kwenu ni mapumziko ya machofu ya kazi? (*Tazama Maelezo ya 78:9*)

10 Na tumeufanya usiku ni sitara kwenu kwa kiza kinacho kufuniki.

11 Na tumeufanya mchana ni wakati wa kuhangaika kwenu kutafuta cha kukusaidieni katika maisha yenu.

12 Na tumesimamisha juu yenu mbingu saba zenye nguvu madhubuti.

13 Na Sisi tumeliumba jua lenye mwangaza na linalo waka. (*Tazama Maelezo 78:13*)

14 Na tumeteremsha kutokana na mawingu yaliyo karibia kunyesha maji yenye kumiminika kwa nguvu. (*Tazama Maelezo 78:14*)

15. Ili tutoe kwayo nafaka na mimea,¹⁵
16. Na mabustani yenye miti iliyo kamatana.¹⁶
17. Hakika siku ya uamuzi imewekewa wakati wake,¹⁷
18. Siku litapo pulizwa barugumu, nanyi mtakuja kwa makundi,¹⁸
19. Na mbingu zitafunguliwa, ziwe milango,¹⁹
20. Na milima itaondolewa na itakuwa kama sarabi.²⁰
21. Hakika Jahannamu inangojea!²¹
22. Kwa walio asi ndio makaazi yao,²²
23. Wakae humo karne baada ya karne,²³
24. Hawataonja humo chochote kibaridi wala kinywaji,²⁴
25. Ila maji yamoto sana na usaha,²⁵
26. Ndio jaza muwafaka.²⁶
27. Hakika hao hawakuwa wakitaraji kuwa kuna hisabu.²⁷
28. Na wakikanusha Aya zetu kwa nguvu.²⁸
29. Na kila kitu Sisi tumekidhibiti kwa kukiandika.²⁹
30. Basi onjeni! Nasi hatutakuzidishi ni ila adhabu!³⁰
31. Hakika wachamngu wanastahiki kufuzu,³¹
32. Mabustani na mizabibu,³²
33. Na wake walio lingana nao,³³
34. Na bilauri zilizo jaa,³⁴
35. Hawatasikia humo upuuzi wala uwongo -³⁵
36. Malipo kutoka kwa Mola wako Mlezi, kipawa cha kutosha.³⁶

15 Ili tutoe kwa maji haya nafaka na mimea kuwa ni chakula kwa ajili ya watu na wanyama.

16 Na mabustani yenye miti iliyo fungamana na matawi yake yameingiliana.

17 Hakika siku ya uamuzi baina ya viumbe imewekewa miadi ilio kwisha kadiriwa kwa ajili ya kufufuliwa.

18 Siku litakapo pulizwa barugumu na kufufuliwa watu, mtakuja kwenye mkutano makundi kwa makundi.

19 Na mbingu zitapasuliwa kila upande hata zitakuwa ni milango milango.

20 Na milima itaondolewa baada ya kung'olewa mwahala mwake, na kuvurugwa, ikawa unaiona kama sura ya milima na hali hiyo ni kifusi tu kilicho rindikwa, kama uonavyo mangati, sarabi, unaona kama sura ya maji nayo si maji.

21 Hakika Jahannamu imekuwa kama ni kitu kinacho ngojea, walinzi wake wanawangojea watu watakao kuja kuingia.

22 Yawe ni marejeo na mafikio kwa wenye kupindukia mipaka ya Mwenyezi Mungu.

23 Watakaa humo dahari baada ya dahari.

24 Hawataonja humo hata chembe ya upepo wa kuburudisha joto lake, wala kinywaji cha kupoza kiu chao.

25 Lakini watakunywa maji yalio pita ukomo kwa umoto wake, na usaha unao miminika kutokana na ngozi za watu wa Motoni.

26 Malipo ya kuwafikiana na vitendo vyao viovu.

27 Kwani hao hawakutaraji kuwa itakuwapo kuhisabiwa, hata watende ya kuwaokoa humo.

28 Wakazikadhibisha Ishara za Mwenyezi Mungu zenye kuthibitisha kufufuliwa kwa mkadhibisho mkali.

29 Na kila kitu tumekidhibiti kwa kukiandika.

30 Basi onjeni, wala hampati kwetu ila kuzidishiwa adhabu tu.

31 Hakika wenye kumcha Mola wao Mlezi watapata kuokoka na adhabu, na wataipata Pepo,

32 Na mabustani yenye matunda, na mizabibu mizuri.

33 Na wanawari walio watipwatipwa wa hirimu yao,

34 Na bilauri safi zilizo jaa pomoni,

35 Hawasikii huko Peponi upuuzi wala uwongo.

36 Ni malipo kutokana na Mola wako Mlezi, kwa fadhila yake na ihsani ya kutosha.

37. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilio baina yao, *Arrahman*, Mwingi wa rehema; hawamiliki usemi mbele yake!³⁷
38. Siku atakapo simama Roho na Malaika kwa safu. Hawatasema ila Mwingi wa rehema aliye mruhusu, na atasema yaliyo sawa tu.³⁸
39. Hiyo ndiyo Siku ya haki. Basi anaye taka na ashike njia arejee kwa Mola wake Mlezi.³⁹
40. Hakika tumekuhadharisheni adhabu iliyo karibu kufika; Siku ambayo mtu atakapo ona yaliyo tangulizwa na mikono yake; na kafiri atasema: Laiti ningeli kuwa udongo!⁴⁰

37 Mola Mlezi wa mbinguni na duniani na vilio baina yao, ambaye rehema yake imeenea juu ya kila kitu. Hapana yeyote mwenye madaraka ya kusema mbele yake.

38 Siku atakapo simama Jibrili na Malaika walio teuliwa nao wamenyenyekea, hasemi mmoja wao ila akipewa idhini na *Arrahman*, Mwingi wa rehema, kuwa aseme, naye atasema lilio sawa tu.

39 Hiyo ndiyo siku isiyo na shaka. Basi atakaye na ashike njia ya kwenda kwa Mola wake Mlezi arejee kwa Imani, na a'mali njema.

40 Hakika Sisi tumekuhadharisheni na adhabu itakayo tokea karibu, siku atakapo angalia mtu vitendo vyake vilivyo tangulizwa na mikono yake, na atakapo sema kafiri kwa kutamani kuokoka: Laiti ningeli bakia udongo baada ya kufa, nisifufuliwe wala nisihisabiwe!

Sura 79 - An-Nazi‘at

Utangulizi

Imeanza Sura hii kwa kiapo juu ya kumkinika kufufuliwa na kutokea kwake, na ikafuatia hayo hadithi ya Musa na Firauni kumliwaza Mtume s.a.w., na ikataja khabari za binaadamu na juhudi zake, na ikadhihirisha yanayo wangojea majabari, na yanayo wangojea makhaini. Na Sura ikakhitimisha kwa kuuliza kwao washirikina lini itakuwa hiyo Saa ya Kiyama, na ikabainisha kwamba kazi ya Mtume ni kuwaonya wenye kukiogopa Kiyama, sio kujua wakati wake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa wanao komoa kwa nguvu,¹
2. Na kwa wanao toa kwa upole,²
3. Na wanao ogelea,³
4. Wakishindana mbio,⁴
5. Wakidabiri mambo.⁵
6. Siku kitapo tetemeka cha kutetemeka,⁶
7. Kifuate cha kufuatia.⁷
8. Siku hiyo nyoyo zitapiga piga,⁸
9. Macho yatainama chini.⁹
10. Sasa wanasema: Ati kweli tutarudishwa kwenye hali ya kwanza?¹⁰
11. Hata tukiwa mifupa iliyo bunguliwa?¹¹
12. Wanasema: Basi marejeo hayo ni yenye khasara!¹²
13. Kwa hakika hayo ni ukelele mmoja tu,¹³

1 Ninaapa kwa kila kilicho pewa uwezo wa kuing'oa vitu kutokana na pahala pao kwa nguvu.

2 Na kwa kila kilicho pewa uwezo wa kuvitoa vitu kwa utaratibu na ulaini,

3 Na kwa kila kilicho pewa mbio za kutekeleza kazi yake kwa sahala na wepesi.

4 Na kwa vinavyo shindania kutimiza waajibu ulio twikwa juu yao kushindania kwa juhudi,

5 Na vinavyo dabiri, kupanga, mambo na kuyaendesha kwa mujibu wa vilivyo khusishwa, bila ya shaka Saa ya Kiyama itafika; hiyo siku ambayo mpulizo wa mwanzo wa barugumu utavitikisa viumbe vyote, na mpulizo huo utafuatiwa na wa pili ambao ndio utakao kuwa wa kufufuliwa watu.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Tazama tanbihi ya 5.

8 Siku hiyo nyoyo zitapatika kwa khofu.

9 Macho ya watu yatakuwa na huzuni, manyonge.

10 Watu hawa husema duniani kwa kukanya kufufuliwa: Ati tutarudishwa sisi baada ya kwisha kufa, tumbwe tena kama tulivyo kuwa?

11 Tukisha kuwa mafupa yaliyo chakaa, ati tutarejeshwa tufufuliwe upya?

12 Wanasema, kwa kukanya na kejeli: Kurejea huko kama kukitokea basi ni marejeo ya khasara, na sisi si watu wa kukhasiri.

13 Msidhani kurejea huko ni kuzito. Kwani hayo ni ukelele mmoja tu, mara maiti wote watahudhurishwa kwenye ardhi ya mkusanyiko!

14. Mara watakuwa kwenye uwanda wa mkutano!¹⁴
15. Je! Imekufikia hadithi ya Musa?¹⁵
16. Mola wake Mlezi alipo mwita katika bonde takatifu la T'uwaa, akamwambia:¹⁶
17. Nenda kwa Firauni. Hakika yeye amezidi jeuri.¹⁷
18. Umwambie: Je! Unapenda kujitakasa?¹⁸
19. Nami nitakuongoa ufike kwa Mola wako Mlezi, upate kumcha.¹⁹
20. Basi alimwonyesha Ishara kubwa.²⁰
21. Lakini aliikadhibisha na akaasi.²¹
22. Kisha alirudi nyuma, akaingia kufanya juhudi.²²
23. Akakusanya watu akanadi.²³
24. Akasema: Mimi ndiye Mola wenu Mlezi mkuu kabisa.²⁴
25. Basi hapo Mwenyezi Mungu akamshika kumuadhibu kwa la mwisho na la mwanzo.²⁵
26. Kwa hakika katika haya yapo mazingatio kwa wanao ogopa.²⁶
27. Je! Ni vigumu zaidi kukuumbeni nyinyi au mbingu? Yeye ndiye aliye ijenga!²⁷
28. Akainua kimo chake, na akaitengeneza vizuri.²⁸
29. Na akautia giza usiku wake, na akautokeza mchana wake.²⁹
30. Na juu ya hivyo ameitandaza ardhi.³⁰
31. Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake,³¹
32. Na milima akaisimamisha,³²
33. Kwa nafuu yenu na mifugo yenu.³³

14 Tazama tanbihi ya 13.

15 Ewe Muhammad! Imekufikilia hadithi ya Musa, alipo mwita Mola wake Mlezi katika bonde lilio takaswa, linalo itwa "T'uwa"?

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Akaambiwa: Nenda kwa Firauni aliye pindukia mpaka katika udhalimu.

18 Umwambie: Je! Huelekei kut'ahirika?

19 Na mimi nikuongoze upate kumjua Mola wako Mlezi, umwogope.

20 Musa akamwonyesha Firauni miujiza mikubwa.

21 Lakini Firauni alimkadhibisha Musa kwa aliyokuja nayo, na akamuasi kwa aliyo mwitia.

22 Kisha akamgeuzia mgongo, akenda kujitahidi kumpinga.

23 Akawakusanya wachawi, na akawaita watu, akasema: Mimi ndiye Mola wenu Mlezi aliye mkubwa kabisa

24 Tazama tanbihi ya 23.

25 Mwenyezi Mungu akampa adhabu kwa kauli yake ya mwisho, nayo ni vile kusema: Mimi ndiye Mola wenu Mlezi aliye mkubwa kabisa. Na akampa adhabu kwa kauli yake ya mwanzo, nayo ni kumkadhibisha Musa a.s.

26 Hakika katika hadithi hiyo yapo mawaidha kwa mwenye kumkhofu Mwenyezi Mungu.

27 Enyi mnao kanya kufufuliwa! Kukuumbeni nyinyi ni taabu zaidi au kuziumba mbingu, kuzikusanya sehemu zake zililo tawanyika mbali mbali, na kunyanyua kimo chake, na zikakaa sawa hazina tafauti wala ila?

28 Tazama tanbihi ya 27.

29 Na akatia kiza katika usiku wake, na akautokeza mchana wake ukawa na mwangaza?

30 Na ardhi baada ya hayo akaikunjua, na akaisawazisha, ikasilihiki kukaliwa na watu wake?

31 Akatoa ndani yake maji yake yanayo tibuka katika chemchem zake, na ikamiminika mito yake, na ikawa na mimea yake ya chakula kwa ajili ya watu na wanyama;

32 Na milima akaithibitisha imara

33 Kwa ajili ya manufaa yenu na wanyama wenu mnao wafuga!

34. Basi itakapo fika hiyo balaa kubwa,³⁴
35. Siku ambayo mtu atakumbuka aliyo yafanya,³⁵
36. Na Jahannamu itadhihirishwa kwa mwenye kuona,³⁶
37. Basi ama yule aliye zidi ujeuri,³⁷
38. Na akakhiari maisha ya dunia,³⁸
39. Kwa hakika Jahannamu ndiyo makaazi yake!³⁹
40. Na ama yule anaye ogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi, na akajizuilia nafsi yake na matamano,⁴⁰
41. Basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makaazi yake!⁴¹
42. Wanakuuliza Saa (ya Kiyama) itakuwa lini?⁴²
43. Una nini wewe hata uitaje?⁴³
44. Kwa Mola wako Mlezi ndio mwisho wake.⁴⁴
45. Kwa hakika wewe ni mwonyaji tu kwa mwenye kuikhofu.⁴⁵
46. Ni kama kwamba wao siku watapo iona (hiyo Saa) hawakukaa ila jioni moja tu, au mchana wake.⁴⁶

34 Kitakapo fika Kiyama ambacho vitisho vyake vitaenea kote,

35 Siku atakapo kumbuka mtu vitendo vyake vya kheri au shari.

36 Na Jahannamu ikadhihirishwa wazi, akaiona kila mwenye macho kuwa ndio malipo,

37 Basi ama mwenye kupita mpaka kwa maasi yake, na akajichagulia nafsi yake maisha yanayo pita njia, basi Moto wa Jahannamu unao babua upepo wake ndio makaazi yake wala hana mengineyo.

38 Tazama tanbihi ya 37.

39 Tazama tanbihi ya 37.

40 Na ama mwenye kukhofu ukubwa na utukufu wa Mola wake Mlezi, na akaizuia nafsi yake na matamano ya kumpumbaza, basi huyo nyumba ya neema ya Peponi ndio makaazi yake, wala hana pengineyo.

41 Tazama tanbihi ya 40.

42 Ewe Muhammad! Wanakuuliza, ati, khabari za Saa ya Kiyama, itakuwa lini?

43 Ujuzi wa hayo hauko kwako hata uwatajije.

44 Ujuzi wa hayo uko kwa Mola wako Mlezi tu, si kwa mwengine. (Nabii Isa a.s. ambaye Wakristo wanasema ni Mwana wa Mungu, au ndiye Mungu, pia anasimuliwa katika Biblia kuwa hakujua Saa na Siku ya Kiyama. Injili ya Mathayo 24.36 inanukulu maneno ya Yesu: "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake.")

45 Kwani waajibu wako ni kuwaonya wanao khofu si kuwatangazia wakati wake.

46 Na wao siku watakayo iona hiyo Saa ya Kiyama ni kama kwamba hawakuishi duniani zaidi kuliko jioni moja tu, au mchana wake.

Sura 80 - 'Abasa

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kumlaumu Nabii Muhammad s.a.w. kwa kumpuuza Ibnu Ummi Maktoum alipo mjia kutafuta ilimu na uwongofu. Naye Nabii s.a.w. alikuwa kashughulika kuwalingania Dini baadhi ya mabwana wa Kikureshi kwa kutaraji watamwitikia, ili kwa kusilimu kwao wange silimu watu wengi. Kisha Sura inamkumbusha binaadamu kwa neema alizo pewa na Mwenyezi Mungu tangu kuumbwa kwake mpaka kufufuliwa kwake. Na ikakhitimisha kwa kusimulia khabari za Siku ya Kiyama, ikibainisha kwamba watu siku hiyo ni makundi mawili, kundi la Waumini lenye furaha, na kundi la makafiri wapotovu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Alikunja kipaji na akageuka,¹
2. Kwa sababu alimjia kipofu!²
3. Na nini kitakujuulisha pengine yeye atatakasika?³
4. Au atawaidhika, na mawaidha yamfae?⁴
5. Ama ajionaye hana haja,⁵
6. Wewe ndio unamshughulikia?⁶
7. Na si juu yako kama hakutakasika.⁷
8. Ama anaye kujia kwa juhudi,⁸
9. Naye anaogopa,⁹
10. Ndio wewe unampuuza?¹⁰
11. Sivyo hivyo! Huku ni kukumbushana.¹¹
12. Basi anaye penda akumbuke.¹²
13. Yamo katika kurasa zilizo hishimiwa,¹³
14. Zilizo inuliwa, zilizo takaswa.¹⁴

1 Uso wake ulitaghayari kwa kuchukua na akageuka,

2 Kwa sababu kamjia kipofu anamuuliza khabari ya Dini yake.

3 Na wewe unajuaje, pengine huyo kipofu atatakasika kwa atayo yapata kwako.

4 Au atawaidhika na mawaidha yamfae.

5 Ama yule anaye jiona ametosheka kwa mali yake na nguvu zake, wewe ndio unamkabili na unamshughulikia kumfikishia wito wako.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Na wewe una lawama gani ikiwa yeye hakutakasika kwa Imani?

8 Ama anaye kukimbilia kutafuta ilimu na uwongofu, naye anamkhofu Mwenyezi Mungu wewe unampuuza.

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Tazama tanbihi ya 8.

11 Hakika Aya hizi ni mawaidha.

12 Mwenye kutaka atawaidhika kwa Qur'ani.

13 Nayo Qur'ani imo katika kurasa zilizo tukuzwa kwa Mwenyezi Mungu.

14 Zina cheo cha juu, na pahala palipo tukuka, zimetakasika na kila upungufu.

15. Zimo mikononi mwa Malaika waandishi,¹⁵
16. Watukufu, wema.¹⁶
17. Ameangamia mwanaadamu! Nini kinacho mkufurisha?¹⁷
18. Kwa kitu gani amemuumba?¹⁸
19. Kwa tone la manii, akamuumba na akamkadiria.¹⁹
20. Kisha akamsahilishia njia.²⁰
21. Kisha akamfisha, akamtia kaburini.²¹
22. Kisha apendapo atamfufua.²²
23. La! Hajamaliza aliyo muamuru.²³
24. Hebu mtu na atazame chakula chake.²⁴
25. Hakika Sisi tumemimina maji kwa nguvu,²⁵
26. Tena tukaipasua pasua ardhi kwa nguvu,²⁶
27. Kisha tukaotesha humo nafaka,²⁷
28. Na zabibu, na mimea ya majani,²⁸
29. Na mizaituni, na mitende,²⁹
30. Na bustani zenye miti iliyo songana baraabara,³⁰
31. Na matunda, na malisho ya wanyama,³¹
32. Kwa manufaa yenu na mifugo yenu.³²
33. Basi utakapo kuja ukelele,³³
34. Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye,³⁴
35. Na mamaye na babaye,³⁵
36. Na mkewe na wanawe -³⁶

15 Katika mikono ya Malaika ambao Mwenyezi Mungu amewafanya ndio mabalozi baina yake na Mitume wake;

16 Walio bora, wema.

17 Ameangamia mwanaadamu! Nini kilicho mfanya akufuru na hali Mwenyezi Mungu amemfanyia hisani zote hizi?

18 Hakumbuki yeye kaumbwa kutokana na nini?

19 Kutokana na maji ya kudharauliwa Yeye Mwenyezi Mungu alimwanzisha kumuumba akamjaalia apitie daraja mbali mbali za kukua.

20 Kisha akamfanyia nyepesi njia ya kufikia Imani, na akamfunza njia hiyo.

21 Kisha akamfisha na akamtukuza kwa kumtia kaburini.

22 Na tena akipenda atamhuisha baada ya kufa kwake.

23 Ni kweli mwanaadamu, juu ya kuwa umri wake mrefu duniani, hakutimiza aliyo amrisha na Mwenyezi Mungu katika mambo ya Imani na ut'iifu.

24 Hebu mtu na aangalie shani ya chakula chake - vipi tulivyo kipanga na kumsahilishia!

25 Ni Sisi tumeiteremsha mvua kutoka mbinguni, ikateremka.

26 Tena tukaipasua pasua ardhi kwa ajili ya mimea.

27 Tukaotesha humo nafaka ambazo watu huzila na huweka akiba.

28 Na mizabibu na mimea ya majani inayo liwa mibichi.

29 Na mizaituni mizuri, na mitende yenye kuzaa,

30 Na mabustani yaliyo songamana matawi ya miti yake,

31 Na matunda ya kustaladhi nayo, na malisha ya kula nyama hoa (mifugo).

32 Tumeotesha yote hayo kwa ajili ya faida yenu na wanyama wenu wa kufuga.

33 Basi utakapo kuja ukelele wa Kiyama utakao tia uziwi masikio.

34 Siku mtu atakapo mkimbia ndugu yake, na mama yake, na baba yake, na mkewe, na wanawe!

35 Tazama tanbihi ya 34.

36 Tazama tanbihi ya 34.

37. Kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na lake la kumtosha.³⁷
38. Siku hiyo ziko nyuso zitazo nawiri,³⁸
39. Zitacheka, zitachangamka;³⁹
40. Na nyuso siku hiyo zitakuwa na mavumbi,⁴⁰
41. Giza totoro litazifunika,⁴¹
42. Hao ndio makafiri watenda maovu.⁴²

37 Kila mmojapo katika hawa atakuwa na jambo lake la kumshughulisha!

38 Zipo nyuso siku hii zenye mwangaza, zenye kung'ara na kufurahi kwa neema za Mwenyezi Mungu.

39 Tazama tanbihi ya 38.

40 Na nyuso nyengine siku hii zina vumbi zimesawijika.

41 Zimegubikwa na kiza na weusi.

42 Wenye nyuso hizi ni makafiri wapotovu, ambao walio kuwa hawabali maasi waliyo kuwa wakiyatenda.

Sura 81 - Attakwir

Utangulizi

Katika Sura hii yanaelezwa yatakayo tokea wakati wa Saa ya Kiyama na baada yake, na yanaelezwa ya kuonyesha dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu, na kutilia mkazo cheo cha Qur'ani tukufu, na kupinga madai ya uzushi katika Qur'ani, na kumtakasa Mtume s.a.w. na tuhuma za wazimu, na kuwatisha na kuwaonya hao wanao endelea na upotovu, na inataka yaangaliwe mazingatio yaliyomo katika Qur'ani ambayo yatawafaa watu wenye kusimama msimamo wa sawa, na inarudisha mambo yote ya watu kwenye mapenzi ya Mola Mlezi wa walimwengu wote.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Jua litakapo kunjwa,¹
2. Na nyota zikazimwa,²
3. Na milima ikaondolewa,³
4. Na ngamia wenye mimba pevu watakapo achwa wasishughulikiwe,⁴
5. Na wanyama wa mwituni wakakusanywa,⁵
6. Na bahari zikawaka moto,⁶
7. Na nafsi zikaunganishwa,⁷
8. Na msichana aliye zikwa hai atapo ulizwa,⁸
9. Kwa kosa gani aliuliwa?⁹
10. Na madaftari yatakapo enezwa,¹⁰
11. Na mbingu itapo tanduliwa,¹¹
12. Na Jahannamu itapo chochewa,¹²
13. Na Pepo ikasogezwa,¹³
14. Kila nafsi itajua ilicho kihudhurisha.¹⁴

1 Jua litakapo kunjwa na mwangaza wake ukafutwa,

2 Na nyota ikazimwa nuru yao,

3 Na milima ikaondoshwa hapo ilipo.

4 Na ambao wa kuchukua mimba wakaharibu mimba zao,

5 Na nyama mwigu wakusanywe kutoka vichakani mwao na mashimoni mwao, hawajijui hawajitambui kwa wingi wa kufazaika.

6 Na bahari zikawa zinawaka moto,

7 Na roho zikaunganishwa na viwiliwili vyao.

8 Na mtoto wa kike aliye zikwa hai, akaulizwa kwa kumliwaza yeye, na kumshutumu aliye mzika hai, kwa makosa gani kauliwa, naye hana dhambi? (Ilikuwa ada ya makafiri wa Kiarabu kabla ya Uislamu kuwazika watoto wao wa kike nao wahai! Baadhi ya Mabaniani wanawauwa watoto wao wa kike hata hivi leo huko India!!)

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Na nyaraka zilizo andikwa ndani vitendo vya watu zikakunjuliwa wakati wa hisabu.

11 Na mbingu itapo ondoshwa pahala pake,

12 Na Moto ukawashwa kwa mwako mkali.

13 Na Pepo ikajongezwa ikawa karibu,

14 Yatakapo tokea yote hayo, basi hapo tena kila nafsi itajua nini iliyo tanguka, ikiwa kheri au shari.

15. Naapa kwa nyota zinapo rejea nyuma,¹⁵
16. Zinazo kwenda, kisha zikajificha,¹⁶
17. Na kwa usiku unapo pungua,¹⁷
18. Na kwa asubuhi inapo pambazuka,¹⁸
19. Kwamba hakika bila ya shaka hii ni kauli ya Mjumbe mtukufu,¹⁹
20. Mwenye nguvu na mwenye cheo kwa huyo Mwenye Kiti cha Enzi,²⁰
21. Anaye t'iiwa, tena muaminifu.²¹
22. Na wala huyu mwenzenu hana wazimu.²²
23. Na hakika yeye alimwona kwenye upeo wa macho ulio safi.²³
24. Wala yeye si bakhili kwa mambo ya ghaibu.²⁴
25. Wala hii si kauli ya Shetani maluuni.²⁵
26. Basi mnakwenda wapi?²⁶
27. Haikuwa hii ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote.²⁷
28. Kwa yule miongoni mwenu anaye taka kwenda sawa.²⁸
29. Wala nyinyi hamtataka isipo kuwa atake Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.²⁹

15 Naapa kiapo cha mkazo kwa nyota ambazo zinanywea zinapo chomoza, na hapo mwanga wake huwa khafifu,

16 Zenye kwenda na hujificha wakati wa kuchwa kwake, kama paa wanapo jificha kwenye mapango yao.

17 Na kwa usiku linapo pungua giza lake wakati unapo malizika.

18 Na kwa asubuhi unapo anza mwangaza wake na ukavuma upepo wake,

19 Hakika Qur'ani bila ya shaka ni kauli ya Mjumbe anaye toka kwa Mwenyezi Mungu, naye ni mwenye kuhishiwa kwake,

20 Mwenye nguvu katika kutekeleza waajibu wake, mwenye cheo na daraja mbele ya Mwenyezi Mungu Mwenye Kiti cha Enzi.

21 Tena ni mwenye kut'iiwa, na muaminifu wa kuchukua wahyi miongoni wa walio juu.

22 Na huyo Mtume wenu ambaye ni mwenzenu, mnaye mjua kuwa ana akili timamu, si mwendawazimu.

23 Na ninaapa kuwa Muhammad s.a.w. bila ya shaka alimwona Jibrili katika upeo wa macho kwa mujibu wa inavyo onekana.

24 Na Muhammad si bakhili wa kufikisha wahyi na kuwafunza watu.

25 Wala huu wahyi (ufunuo) ulio teremshwa juu yake si kauli ya Shetani aliye fukuzwa kutoka kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu.

26 Basi njia gani iliyo ya uwongofu zaidi kuliko hii mnayo ifuata?

27 Qur'ani si chochote ila ni ukumbusho na mawaidha kwa walimwengu wote.

28 Kwa anaye taka, miongoni mwenu, kusimama sawa kufikilia haki na kweli.

29 Na nyinyi hamwezi kutaka kitu ila anapo taka Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.

Sura 82 - Al-Infit'aar

Utangulizi

Sura hii imeeleza baadhi ya vitisho vya Saa ya Kiyama kwa njia ya kutangaza kuwa hakika litatokea jambo katika siku ambayo kila mtu atajua nini alilo litanguliza na nini alilo liakhirisha. Tena Aya zikaingia kumhadharisha mwanaadamu aliye danganyika na Mola wake Mlezi aliye muumba akamweka sawa, akamjenga kwa namna ya pekee, na kwa umbo bora kabisa. Inathibitisha Sura kuwa huyo mtu anaikadhibisha Siku ya Malipo, na inatilia mkazo kuwepo Malaika juu yake, walinzi mahashumu, waandishi. Na ikamalizia kusema kuwa watu wema watapata neema. Na wapotovu hawatapata ila Jahannamu, watakayo iingia Siku ya Kiyama, siku ambayo nafsi haitoweza kuimilikia nafsi nyengine chochote. Na amri yote itakuwa ni ya Mwenyezi Mungu tu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Mbingu itapo chanika,¹
2. Na nyota zitapo tawanyika,²
3. Na bahari zitakapo pasuliwa,³
4. Na makaburi yatapo fukuliwa,⁴
5. Hapo kila nafsi itajua ilicho tanguliza, na ilicho bakisha nyuma.⁵
6. Ewe mwanaadamu! Nini kilicho kughuri ukamwacha Mola wako Mlezi Mtukufu?⁶
7. Aliye kuumba, akakuweka sawa, akakunyoocha,⁷
8. Katika sura yoyote aliyo ipenda akakujenga.⁸
9. Sivyo hivyo! Bali nyinyi mnaikanusha Siku ya Malipo.⁹
10. Na hakika bila ya shaka wapo walinzi juu yenu,¹⁰
11. Waandishi wenye hishima,¹¹
12. Wanayajua mnayo yatenda.¹²
13. Hakika wema bila ya shaka watakuwa katika neema,¹³

1 Itakapo pasuka mbingu,

2 Na nyota zitakapo pukutika na kutawanyika,

3 Na bahari zikafurika na kuingiliana kwa kuondoka viziwizi baina yao,

4 Na makaburi yakafunuliwa na wakatoka maiti walio kuwamo.

5 Hapo basi kila nafsi itajua nini kheri au shari iliyo tanguliza na iliyo chelewesha.

6 Ewe mwanaadamu! Kitu gani kilicho kukhadaa wewe na Mola wako Mlezi Mtukufu hata ukafanya jeuri ya kwenda kumuasi? (*Tazama Maelezo 82:6*)

7 Mungu wako huyo ndiye aliye kuumba nawe hukuwa chochote, akakuumba na viungo vya kukuletea manufaa, akakufanya umenyooka kwa umbo sawa sawa.

8 Akakujenga na akakuleta katika sura yoyote aliyo itaka.

9 Hamwachi? Bali nyinyi mnakadhibisha malipo ya Siku ya Kiyama!

10 Na hakika wapo juu yenu Malaika walinzi, ambao ni waheshimiwa kwetu, wanasajili vitendo vyenu vyote mvitendavyo, vya kheri na shari.

11 Tazama tanbihi ya 10.

12 Tazama tanbihi ya 10.

13 Hakika wale walio ni wa kweli katika Imani yao wapo katika neema kubwa.

14. Na hakika waovu bila ya shaka watakuwa Motoni;¹⁴
15. Wataingia humo Siku ya Malipo.¹⁵
16. Na hawatoacha kuwamo humo.¹⁶
17. Na nini kitakacho kujuulisha Siku ya Malipo ni siku gani?¹⁷
18. Tena nini kitakacho kujuulisha Siku ya Malipo ni siku gani?¹⁸
19. Siku ambayo nafsi haitakuwa na madaraka yoyote juu ya nafsi; na amri yote siku hiyo ni ya Mwenyezi Mungu tu.¹⁹

14 Na hakika walio iacha amri ya Mwenyezi bila ya shaka watakuwa katika Moto unao unguza, wataingia humo Siku ya Malipo.

15 Tazama tanbihi ya 14.

16 Na wala hawatatoka katika Jahannamu!

17 Na nini kitakujuvya ni nini hiyo Siku ya Malipo, na mambo yake yamepindukia ujuzi wako na fikra zako?

18 Tena ni nini kitakacho kujuvya ni nini hiyo Siku ya Malipo kwa vitisho vyake na shida zake?

19 Siku ambayo nafsi haitakuwa na mamlaka yoyote juu ya nafsi ya kuifaa au kuidhuru; na amri yote siku hiyo itakuwa ni ya Mwenyezi Mungu peke yake!

Sura 83 - Al-Mut'affi'in

Utangulizi

Imeanzia Sura hii kwa onyo kali kwa huyo anaye jipimia mwenyewe sawa na akampimia mtu mwingine kwa upungufu; na ikaeleza hayo kwa wayatendayo watu katika kutaka watimiziwe haki zao katika vipimo na mizani, na ikaonya mtindo kama huo kwa kuwa ipo Siku ya Hisabu, na ikathibitisha kuwa vitendo vyao vimedhibitiwa katika daftari la hisabu, ambalo halimkadhibishi ila mwenye kupindukia mipaka, mwenye dhambi aliye zuiliwa na rehema za Mola wake Mlezi, na mwisho wake ni Jahannamu.

Tena Aya zikawageukia watu wema, zikawatuza nyoyo kwa vitendo vyao, na zikataja neema zao na alama zao, zikiashiria namna moja wapo katika neema hizo, na kwa ajili ya hizo washindanie wanao shindana. Na Aya zikaeleza walio kuwa wakiyafanya makafiri wakosefu kuwafanyia Waumini wanapo waona, au wanapo kuwa Waumini wanapita mbele yao. Na Sura ikakhitimisha kwa kuwatuliza Waumini kwamba Siku ya Kiyama itawafanyia insafu, wao watakuwa katika neema wakiwacheka makafiri, nao wamekaa juu ya makochi wakiwaangalia, na makafiri watalipwa kwa waliyo kuwa wakiyatenda.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ole wao hao wapunjao!¹
2. Ambao wanapo jipimia kwa watu hudai watimiziwe.²
3. Na wao wanapo wapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza.³
4. Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa⁴
5. Katika Siku iliyo kuu,⁵
6. Siku watapo msimamia watu Mola Mlezi wa walimwengu wote?⁶
7. Hasha! Hakika maandiko ya wakosefu bila ya shaka yamo katika Sijin.⁷
8. Unajua nini Sijin?⁸
9. Kitabu kilicho andikwa.⁹
10. Ole wao siku hiyo kwa wanao kadhibisha!¹⁰

1 Wataangamia wanao punja, ambao wakijipimia wenyewe kwa watu hujitwalia ya kutosha na kuzidi, na wakiwapimia watu kwa vipimo au mizani huwapunguzia haki yao wanayo stahiki, kwa dhulma!

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Tazama tanbihi ya 1.

4 Hivyo haiwapitikii katika akili zao hawa wanao punja wenzao kwamba watakuja fufuliwa katika siku ya vitisho vikuu?

5 Tazama tanbihi ya 4.

6 Siku watapo simama watu kwa amri ya Mola Mlezi wa walimwengu wote na hukumu yake?

7 Wacheni kupunja, na kughafilika na kufufuliwa! Kwani hakika waliyo andikiwa wakosefu katika a'mali zao mbovu, bila ya shaka yamo katika Sijin.

8 Na nini kitakujavya nini hiyo Sijin?

9 Hicho ni Kitabu kilicho pigwa mistari baina ya maandishi yake.

10 Wataangamia wanao kadhibisha siku itapo kuwa kufufuliwa na kuhisabiwa.

11. Ambao wanaikadhibisha Siku ya Malipo.¹¹
12. Wala haikadhibishi ila kila mwenye kuruka mipaka, mwenye dhambi.¹²
13. Anapo somewa Aya zetu husema: Ni visa vya watu wa kale!¹³
14. Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao hao walio kuwa wakiyachuma.¹⁴
15. Hasha! Hakika hao siku hiyo bila ya shaka watazuiliwa na neema za Mola wao Mlezi.¹⁵
16. Kisha wataingia Motoni!¹⁶
17. Kisha waambiwe: Haya ndiyo mliyo kuwa mkiyakadhabisha.¹⁷
18. Hasha! Hakika maandiko ya watu wema bila ya shaka yamo katika I'liyyin.¹⁸
19. Na nini kitakacho kujuvya nini I'liyyin?¹⁹
20. Kitabu kilicho andikwa.²⁰
21. Wanakishuhudia walio karibishwa.²¹
22. Hakika watu wema bila ya shaka watakuwa katika neema.²²
23. Wakae juu ya viti vya enzi wakiangalia.²³
24. Utatambua katika nyuso zao mng'aro wa neema,²⁴
25. Watanyweshwa kinywaji safi kiliyo tiwa muhuri,²⁵
26. Muhuri wake ni miski. Na katika hayo washindanie wenye kushindana.²⁶
27. Na mchanganyiko wake ni Tasniim,²⁷
28. Chemchem watakayo inywa walio kurubishwa.²⁸
29. Kwa hakika wale walio kuwa wakosefu walikuwa wakiwacheka walio amini.²⁹

11 Ambao wanaikanusha Siku ya Malipo.

12 Na wala haikanushi Siku ya Malipo ila kila mwenye kupindukia mipaka mwingi wa madhambi.

13 Na akisomewa Aya za Mwenyezi Mungu zenye kutaja kuwepo malipo husema: Huo ni uwongo wa walio tangulia!

14 Ewe uliye kiuka mipaka! Wacha kauli hiyo potovu. Bali nyoyo za wenye kupindukia mipaka imegubikwa na ukafiri na maasi waliyo yatenda.

15 Hakika ni kweli kuwa hao wanao kadhibisha watazuiliwa siku hiyo rehema ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya maasi waliyo yachuma.

16 Kisha hakika hao bila ya shaka wataingia Motoni.

17 Kisha wataambiwa kwa kuwakebehi: Hii basi ndiyo adhabu inayo kuteremkieni ambayo mlikuwa mkiikanusha duniani!

18 Ni hakika kuwa vitendo vya watu wema bila ya shaka vimeandikwa katika I'liyyin.

19 Na nini cha kukujuvya nini I'liyyin?

20 Hicho ni Kitabu kilicho andikwa wazi maandishi yake, wanakihudhuria na kukihifadhi Malaika walio kurubishwa.

21 Tazama tanbihi ya 20.

22 Hakika watu wema bila ya shaka watakuwa katika neema za Peponi, juu ya viti vya enzi, wakiziangalia neema na ukarimu alio wakirimu Mwenyezi Mungu.

23 Tazama tanbihi ya 22.

24 Utaona katika nyuso zao uchangamfu na mng'aro wa neema.

25 Wakinyweshwa kinywaji safi kilicho hifadhiwa; kuhifadhiwa huko hakukuzidisha ila uzuri wake. Na kupata neema hizo, basi, na washindanie wanao shindana.

26 Tazama tanbihi ya 25.

27 Cha kuchanganyia kinywaji hicho ni maji ya Tasniim ya Peponi, nayo ni chemchem wanao inywa walio kurubishwa si wengineo, katika watu wa Peponi.

28 Tazama tanbihi ya 27.

29 Wale walio kuwa wakibeba madhambi kuipingia Dini walikuwa wakiwacheka kuwakejeli Waumini duniani

30. Na wanapo pita karibu yao wakikonyezana.³⁰
31. Na wanapo rudi kwa watu wao hurudi nao wamefurahi.³¹
32. Na wanapo waona husema: Hakika hawa ndio khasa walio potea.³²
33. Na wao hawakutumwa wawe walinzi juu yao.³³
34. Basi leo walio amini ndio watawacheka makafiri,³⁴
35. Nao wako juu ya viti vya enzi wakiangalia.³⁵
36. Je! makafiri wamelipwa malipo ya yale waliyo kuwa wakiyatenda?³⁶

30 Na wakiwapa Waumini mbele yao basi wao hukonyezana kwa kuwabeza.

31 Na hao wakosefu wakirejea kwa ahali zao hurejea kwa furaha na kuona ladha kwa vile kuwakejeli Waumini.

32 Na wakiwaona Waumini husema: Ama hakika hawa wamepotea kweli kwa kumuamini Muhammad. Wala hao wakosefu hawakutumwa wawe wa kuwahukumu Waumini kwa kuwaongoza au kuwapoteza, wala kuwa ni walinzi wa vitendo vyao.

33 Tazama tanbihi ya 32.

34 Basi Siku ya Malipo walio amini watakuwa ndio wa kuwacheka hao makafiri kwa kuwalipizia kile kicheko chao na kejeli yao ya duniani.

35 Ilhali wako juu ya vitanda na matakuwa watakuwa Waumini wakiziangalia neema za Mwenyezi Mungu alizo wapa.

36 Je! Makafiri watalipwa huko Akhera kwa waliyo yatenda duniani?

Sura 84 - Al-Inshiqaaq

Utangulizi

Sura hii imetaja baadhi ya ishara za Saa ya Kiyama, na kunyenyekea ardhi na mbingu kufuata atakavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na imefahamisha kwamba mtu anachungwa ende akakutane na Mola wake Mlezi, na kwamba vitendo vyake vimeandikwa katika daftari atakalo kuja likuta. Basi mwenye kulipokea kwa mkono wake wa kulia, hisabu yake itakuwa nyepesi. Na mwenye kulipokea kwa mkono wa kushoto atayayatika kuipata adhabu na kuingia Motoni. Tena Mwenyezi Mungu *Subhanahu* ameapa kwa Ishara ambazo zinashuhudia uweza wake, na ambazo zinaitia imani ya kufufuliwa. Lakini juu ya hayo walio kufuru hawaamini, wala hawaizingatii Qur'ani, wala hawazifuati hukumu zake. Kisha Sura inakhitimisha kwa kuonya kwamba Mwenyezi Mungu anayajua wanayo dhamiria, na kwamba Yeye amekwisha waandalia adhabu iliyo chungu, kama alivyo waandalia Waumini ujira wa daima usio katika.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Itapo chanika mbingu,¹
2. Na ikamsikiliza Mola wake Mlezi, na ikapasiwa kumsikiliza,²
3. Na ardhi itakapo tanuliwa,³
4. Na kuvitoe vilivyo kuwa ndani yake, ikawa tupu,⁴
5. Na ikamsikiliza Mola wake Mlezi, na ikapasiwa kumsikiliza,⁵
6. Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumwendea Mola wako Mlezi, basi utamkuta.⁶
7. Ama atakaye pewa daftari lake kwa mkono wa kulia,⁷
8. Basi huyo atahisabiwa hisabu nyepesi,⁸
9. Na arudi kwa ahali zake na furaha.⁹
10. Na ama atakaye pewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake,¹⁰

1 Mbingu itapo chanika, ikaamrisha iondoke,

2 Na ikamsikiliza Mola wake Mlezi na ikamt'ii, na ndio maelekeo yake isikie na kut'ii,

3 Na ardhi ikazidi upana wake kwa kulazwa milima na kuondolewa kifusi chake,

4 Na ardhi ikatoa nje maiti na khazina ziliyo kuwamo ndani yake, na ikaachana navyo vyote hivyo.

5 Na ikamwelekea Mola wake Mlezi kwa kuzidi kutanuka kwake na kutoa vilio kuwemo ndani yake na kuachana navyo, na hayo ni haki yake kuwa. Yakitokea yote hayo yaliyo tangulia kusimuliwa basi kila mtu atapata malipo ya vitendo vyake.

6 Ewe mtu! Hakika wewe unafanya juhudi katika vitendo vyako vikufikishie lengo lako. Basi utakuja kukutana na Mola wako Mlezi kwa a'mali yako, naye atakulipa kwayo.

7 Ama mwenye kupewa daftari la vitendo vyake kwa mkono wake wa kulia basi atahisabiwa kwa hisabu nyepesi, na atarejea kwa jamaa zake Waumini naye furahani.

8 Tazama tanbihi ya 7.

9 Tazama tanbihi ya 7.

10 Ama mwenye kupewa daftari lake kwa mkono wa kushoto wake nyuma ya mgongo wake kwa kudharauliwa shani yake, huyo atatamani ajiue, na ataingia Motoni aungulie mbali!

11. Basi huyo ataomba kuteketea.¹¹
12. Na ataingia Motoni.¹²
13. Hakika alikuwa furahani kati ya jamaa zake.¹³
14. Huyo hakika alidhani kuwa hatarejea tena.¹⁴
15. Kwani? Hakika Mola wake Mlezi alikuwa akimwona!¹⁵
16. Basi ninaapa kwa wekundu wa jua linapo kuchwa,¹⁶
17. Na kwa usiku na unavyo vikusanya,¹⁷
18. Na kwa mwezi unapo pevuka,¹⁸
19. Lazima mtapanda t'abaka kwa t'abaka!¹⁹
20. Basi wana nini hawaamini?²⁰
21. Na wanapo somewa Qur'ani hawasujudu?²¹
22. Bali walio kufuru wanakanusha tu.²²
23. Na Mwenyezi Mungu anajua wanayo yadhamiria.²³
24. Basi wabashirie adhabu chungu!²⁴
25. Isipo kuwa wale walio amini na wakatenda mema; hao watakuwa na ujira usio malizika.²⁵

11 Tazama tanbihi ya 10.

12 Tazama tanbihi ya 10.

13 Kwani huyo hakika duniani alikuwa furahani kati ya jamaa zake akitanaamu na pumbao alilo kuwa nalo hata akapuza a'mali ya kuitenda kwa mustakabali wake.

14 Hakika huyo alidhani kuwa kabisa hatorejea kwa Mwenyezi Mungu akamhisabu.

15 Bali atarejea, na atahisabiwa! Kwani Mola wake Mlezi alikuwa anamwona vyema yeye na vitendo vyake.

16 Basi naapa kiapo cha mkazo kwa wekundu wa mbingu baada ya kuchwa jua.

17 Na kwa usiku na unavyo vikusanya vyote katika giza lake, wanaadamu, wanyama na vyenginevyo!

18 Na mwezi unapo kamilika kupevuka na kutimia nuru yake, hapana shaka yoyote mtakutana na hali baada ya hali, baadhi yake zina shida zaidi kuliko nyenginezo, za kufa na kufufuliwa na vitisho vya Kiyama.

19 Tazama tanbihi ya 18.

20 Wana nini hawa makafiri yanayo wazuia wasimuamini Mwenyezi Mungu na kufufuliwa baada ya kuwekwa wazi dalili zake zote za kuwajibika kwake?

21 Na pindi wakizisikia Aya za Qur'ani hawasujudu wakanyenyekoa?

22 Bali watu hawa, kwa ukafiri wao, wanakanusha kwa inadi na kutakabari kuikataa Haki!

23 Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kabisa hayo wanayo yadhamiria katika nyoyo zao.

24 . Basi wabashirie, kwa kejeli, kuwa watapata adhabu ya kutia uchungu.

25 Lakini walio amini na wakatenda mema watapata, kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ujira usio wakatikia na wala usio kuwa na hisabu juu yao.

Sura 85 - Al-Buruuj

Utangulizi

Sura hii ni ya maliwaza na kuwapa mawaidha Waumini, na kuwatisha na kuwaonya wenye inadi. Imeanzia kwa kiapo chake Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa madhaahiri yanayo onekana ya uweza wake ya kwamba wapinzani wanao waudhi Waumini watafukuzwa kwenye uwanja wa rehema, kama walivyo fukuzwa walio kwenda mwendo wao katika mataifa yaliyo tangulia. Na Sura ikaingia kusimulia kisa cha hao majabari walivyo watendea Waumini, na ikafuatiza kwa kuwapa ahadi Waumini na kuwakhofisha majeuri, na kwamba Haki katika kila zama hupingwa na wapinzani. Na kwamba Qur'ani, ambayo ndiyo mwega wa Haki, na wangaikadhibisha watu fulani, lakini hiyo iko mbali kabisa na shaka, kwa sababu hakika hiyo iko katika *Lauh'un Mahfuudh*, Ubao Ulio Hifadhiwa ulioko kwa Mwenyezi Mungu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa mbingu yenye Buruji!¹
2. Na kwa siku iliyo ahidiwa!²
3. Na kwa shahidi na kinacho shuhudiwa!³
4. Wameangamizwa watu wa makhandaki!⁴
5. Yenye moto wenye kuni nyingi,⁵
6. Walipo kuwa wamekaa hapo,⁶
7. Na wao ni mashahidi wa yale waliyo kuwa wakiwafanyia Waumini.⁷
8. Nao hawakuona baya lolote kwao ila kuwa wakimuamini Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Msifiwa,⁸
9. Ambaye anao ufalme wa mbingu na ardhi; na Mwenyezi Mungu ni shaahidi wa kila kitu.⁹
10. Hakika walio wafitini Waumini wanaume na Waumini wanawake, kisha hawakutubu, basi watapata adhabu ya Jahannamu na watapata adhabu ya kuungua.¹⁰

1 Naapa kwa mbingu yenye Buruj au Manaazil, njia au vituo ambavyo nyota hupitia katika nyendo zake. (*Tazama Maelezo 85:1*)

2 Na kwa Siku iliyo ahidiwa kuwa ndiyo Siku ya Hisabu na Malipo,

3 Na kwa viumbe watao hudhuria Siku hiyo wakaona vitisho na ajabu zitakazo kuwepo,

4 Hakika Mwenyezi Mungu amewalaani watu walio chimba khandaki katika ardhi,

5 Wakawasha moto kuwatumbukiza ndani yake Waumini ili kuwatesa,

6 Na wao wamekaa ukingoni mwake wakashuhudia mateso yanayo wapata Waumini.

7 Na wao wapo hapo wamehudhuria kwenye mateso wanayo watendea Waumini.

8 Na hapana walilo lichukia kwa hao Waumini ila ni kuwa wakimuamini Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu ambaye adhabu yake huogopwa, Msifiwa anaye tarajiwa thawabu zake.

9 Ambaye, peke yake, ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni shahidi anashuhudia yote wayatendayo Waumini na makafiri na atawalipa kwayo.

10 Hakika walio watia matatani Waumini wanaume na Waumini wanawake kwa maudhi na kuwaadhibu kwa moto, kisha wasitubu na kurejea nyuma watapata Akhera adhabu ya Jahannamu kwa ukafiri wao, na watapata adhabu ya kuunguzwa kwa kule kuwaunguza moto Waumini.

11. Hakika walio amini na wakatenda mema watapata Bustani zenye mito ipitayo kati yake. Huko ndiko kufuzu kukubwa.¹¹
12. Hakika kutesa kwa Mola wako Mlezi ni kukali.¹²
13. Yeye ndiye anaye anzisha na ndiye anaye rejeza tena,¹³
14. Naye ni Mwenye kusamehe, Mwenye mapenzi,¹⁴
15. Mwenye Kiti cha Enzi, Mtukufu,¹⁵
16. Atendaye ayatakayo.¹⁶
17. Je! Zimekuwasilia khabari za majeshi?¹⁷
18. Ya Firauni na Thamudi?¹⁸
19. Lakini walio kufuru wamo katika kukadhibisha.¹⁹
20. Na Mwenyezi Mungu nyuma yao amewazunguka.²⁰
21. Bali hii ni Qur'ani tukufu²¹
22. Katika Ubao Ulio Hifadhiwa.²²

11 Hakika hao walio kusanya kwenye Imani ya Mwenyezi Mungu vitendo vyema watapata Mabustani yapitayo mito kati yake. Neema hiyo waliyo lipwa ni kufuzu kukubwa.

12 Hakika mshiko wa Mola wako Mlezi kuwashika majabari umefika ukomo kwa ukali wake

13 Ni Yeye peke yake ndiye Mwenye kuanza kuumba, na kisha ni Yeye anaye rejeza tena,

14 Na Yeye ni Mwingi wa msamaha kwa mwenye kutubu na akarejea, na Mwingi wa mapenzi kwa mwenye kumpenda na akamt'ii.

15 Yeye ndiye Mwenye Kiti cha Enzi na Mwenye kukimiliki, na Mkuu kwa dhati yake na sifa zake.

16 Ni Mtendaji kwa alitakalo, na hendi kinyume na uweza wake yeyote anaye taka.

17 Je! Imekujia, ewe Muhammad, hadithi ya kile kikundi kilicho a'si katika mataifa yaliyo kwisha pita?

18 Kaumu ya Firauni na Thamudi na yaliyo washukia katika malipo ya kushikilia kwao upotovu?

19 Bali hao makafiri katika kaumu yako ni shadidi zaidi katika kukukadhibisha kuliko hawa walivyoo wakadhibisha Mitume wao.

20 Na Mwenyezi Mungu anawaweza hao, na anawajua vilivyo.

21 Bali hii ulio waletaa ni Qur'ani tukufu inadhihirisha hoja za ukweli wako.

22 Imo katika Ubao Ulio Hifadhiwa, hapana uwezo unao weza kuiptoa au kuigeuza.

Sura 86 - Att'aariq

Utangulizi

Sura hii imeanzia kwa kiapo cha kuashiria dalili za kudra ya Mwenyezi Mungu, na inatilia mkazo kuwa kila nafsi ina mlinzi wake na muangalizi, na inamtaka mtu ajifikirie kuumbwa kwake, na ya kwamba yeye kaumbwa na maji yenye kutoka kwa kasi, ili ipatikane hoja kwamba Mwenye kuumba hivi ni Mweza wa kumrejeza tena baada ya kufa kwake. Tena ikaapa mara ya pili kwamba Qur'ani ni kauli ya kufafanua wala si maneno ya maskhara. Na juu ya kuwa hivyo makafiri bila ya shaka wameshughulika kuikanya na kuipangia njama. Na Mwenyezi Mungu amezirudi njama zao kwa njama kali kuliko zao. Kisha Sura imekhitimisha kwa kutaka wapewe muhula makafiri.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa mbingu na Kinacho kuja usiku!¹
2. Na nini kitakacho kujuulisha ni nini hicho Kinacho kuja usiku?²
3. Ni Nyota yenye mwanga mkali.³
4. Hapana nafsi ila inayo mwangalizi.⁴
5. Hebu naajitazame mwanaadamu ameumbwa kwa kitu gani?⁵
6. Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa,⁶
7. Yatokayo baina ya mifupa ya mgongo na mbavu.⁷
8. Hakika Yeye ana uweza wa kumrudisha.⁸
9. Siku zitakapo dhihirishwa siri.⁹
10. Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi.¹⁰
11. Naapa kwa mbingu yenye marejeo!¹¹
12. Na kwa ardhi inayo pasuka!¹²
13. Hakika hii ni kauli ya kupambanua.¹³

1 Naapa kwa mbingu na nyota inayo tokeza usiku!

2 Na kitu gani kitakujuyva ukweli wa nyota hii? Ni hiyo inayotoa mwanga wake katika giza.

3 Tazama tanbihi ya 2.

4 Hapana nafsi ila inayo mlinzi wa kuiangalia na kudhibiti vitendo vyake.

5 Basi naafikiri mtu, yeye kaumbwa kutokana na nini?

6 Ameumbwa mtu kutokana na maji yanayo toka kwa nguvu.

7 Maji haya yanatoka baina ya uti wa mgongo na mbavu za mwanamume na mwanamke. (*Tazama Maelezo 86:7*)

8 Hakika Mwenyezi Mungu aliye muumba hivi hapo mwanzo, bila ya shaka ni Muweza wa kumuumba tena baada ya kufa kwake.

9 Siku dhamiri zitapo fanyiwa mtihani, na zitengwe mbali mbali baina ya ziliyo kuwa nzuri na ziliyo kuwa mbovu.

10 Basi hapana mtu wakati huo ataye kuwa na nguvu ya kujikinga nafsi yake, wala hatakuwa na msaidizi wa kumnusuru.

11 Naapa kwa mbingu yenye mvua inayo rejea na kuja mara kwa mara!

12 Na ardhi inayo pasuka kwa kuchipuka mimea!

13 Hakika hii Qur'ani ni yenye kupambanua baina ya kweli na uwongo. Wala haina nuksani yoyote ya mchezo au maskhara.

14. Wala si mzaha.¹⁴

15. Hakika wao wanapanga mpango.¹⁵

16. Na Mimi napanga mpango.¹⁶

17. Basi wape muhula makafiri - wape muhula pole pole.¹⁷

14 Tazama tanbihi ya 13.

15 Hakika hao wanao ikadhibisha Qur'ani wanaipangia njama kutaka kuiharibia, njama zenye kufikia ukomo!

16 Lakini Mimi nitawalipa, na nitavipambanisha hivyo vitimbi vyao kwa vitimbi madhubuti ambavyo hawataweza kujikinga navyo.

17 Basi wangojee hao makafiri! Wape muhula wa karibu mpaka nikuamrishe amri gani kali ya kuwatendea.

Sura 87 - Al-A‘alaa

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kumtakasa huyo aliye umba vitu vyote, na akavifanya vyote sawa kwa kuvishughulikia, na akakadiria kila kitu kwa kinavyo silihi, basi akakiongoza kifikilie hivyo. Na akaotesha malisho ya wanyama, na khalafu akayafanya makavu yaliyo ingia weusi. Kisha Aya zikatoa khabari kwamba Mwenyezi Mungu atamsomesha Mtume wake Qur’ani, naye ataihifadhi, wala hatosahau chochote katika hivyo ila apende Mwenyezi Mungu. Na atamsahilishia kwa wepesi. Kisha Sura inamuamrisha Mtume akumbushe kwa Qur’ani apate kukumbuka mwenye kuogopa, na ajitenge na ukumbusho huyo mwovu atakaye ingia kwenye Moto mkubwa. Na Aya zimetilia mkazo kwamba uwokovu ni wa mwenye kujisafisha, na akalikumbuka jina la Mola wake Mlezi, na akasali. Na Sura imekhitimisha kwa kubaini kwamba yaliyo kuja humu yamethibiti katika Vitabu vya zamani, Vitabu vya Ibrahimu na Musa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Litakase jina la Mola wako Mlezi aliye juu kabisa,¹
2. Aliye umba, na akaweka sawa,²
3. Na ambaye amekadiria na akaongoa,³
4. Na aliye otesha malisho,⁴
5. Kisha akayafanya makavu, meusi.⁵
6. Tutakusomesha wala hutasahau,⁶
7. Ila akipenda Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye anayajua yaliyo dhaahiri na yaliyo fichikana.⁷
8. Na tutakusahilishia yawe mepesi.⁸
9. Basi kumbusha, kama kukumbusha kunafaa.⁹
10. Atakumbuka mwenye kuogopa.¹⁰
11. Na atajitenga mbali nayo mpotovu,¹¹
12. Ambaye ataingia Moto mkubwa.¹²

1 Litakase jina la Mola wako Mlezi lilio tukufu na kila kitu kisicho kuwa kinaelekeana nalo.

2 Aliye umba kila kitu, na akajaalia uumbaji wote sawa sawa katika hukumu na kupangana.

3 Na akakadiria kwa kila kitu kwa mujibu wa maslaha yake, na akakiongoza.

4 Na ambaye akatoa kwenye ardhi mimea namna mbali mbali ya kuwalisha wanyama.

5 Na akaifanya mimea hiyo baada ya kuwa kijani imestawi, ikakauka na imekuwa myeusi!

6 Ewe Muhammad! Sisi tutakujaalia uwe ni mwenye kuisoma Qur’ani kwa ufunuo kutoka kwetu, na wala hutasahau utacho kihifadhi.

7 Isipo kuwa anacho taka Mwenyezi Mungu ukisahau, kwani hakika Yeye Mtukufu anayajua wanayo yadhihirisha waja wake na wanayo yaficha, ikiwa maneno au vitendo.

8 Na tutakuwezesha kupita njia ya kufikilia kwa wepesi mambo yako yote.

9 Basi wakumbushe watu ikiwa kukumbusha kutaleta manufaa, kwani inavyo faa ndio kuwanafisha.

10 Watanafiika kwa ukumbusho wako wanao mwogopa Mwenyezi Mungu.

11 Na atajitenga na ukumbusho mpotovu anaye shikilia kufanya inda na ukafiri.

12 Ambaye ataingia kwenye Moto mkubwa ulio andaliwa kuwa ndio malipo yake.

13. Tena humo hatakufa wala hawi hai.¹³
14. Hakika amekwisha fanikiwa aliye jitakasa.¹⁴
15. Na akakumbuka jina la Mola wake Mlezi, na akasali.¹⁵
16. Lakini nyinyi mnakhiari maisha ya dunia!¹⁶
17. Na Akhera ni bora na yenye kudumu zaidi.¹⁷
18. Hakika haya yamo katika Vitabu vya mwanzo,¹⁸
19. Vitabu vya Ibrahimu na Musa.¹⁹

13 Tena hatokufa huko Motoni akapumzika kwa kifo, wala hawi hai kwa uhai wa kustarehe nao.

14 Hakika amefuzu mwenye kujisafisha na ukafiri na maasi.

15 Na akalikumbuka jina la Muumba wake kwa moyo wake na ulimi wake, na akasali kwa unyenyekevu kama itakikanavyo.

16 Bali nyinyi hamfanyi hayo yanayo pelekea kufanikiwa, lakini katika hima zenu mnatanguliza maisha ya duniani kuliko ya Akhera.

17 Na Akhera ni bora kuliko dunia, kwa usafi wa neema zake, na ni yenye kubaki na kudumu zaidi.

18 Hakika haya yote yaliyo tajwa katika Sura hii bila ya shaka yamethibitishwa katika Vitabu vya zamani, Vitabu vya Ibrahimu na Musa; kwani haya yamewafikiana na mafunzo ya dini zote na yamesajiliwa katika Vitabu vya mbinguni.

19 Tazama tanbihi ya 18.

Sura 88 - Al-Ghaashiyah

Utangulizi

Imeanza Sura hii kwa njia ya kutia shauku kuisikiliza hadithi ya Siku ya Kiyama, na hayo mambo yatakayo tokea humo. Inaashiria kwamba watu ni makundi mawili: miongoni mwao wapo ambao hawatapata hishima yoyote kwa watakavyo pokewa na wataingia kwenye Moto mkali. Na wapo watakao ifikia siku hiyo kwa furaha kwa namna ya rehema na radhi zilizo andaliwa kwa ajili yao. Kisha Sura ikaeleza dalili zilizo wazi za uweza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kufufua kutokana na wanavyo ona wenyewe kwa macho yao na wanayo nafika kwayo katika uhai wao. Na baada ya kuzitaja dalili hizi ikageukia khabari za Mtume s.a.w. kwa kukumbusha kwamba waajibu wake mkubwa kwa mintarafu yao ni wazi, ya kwamba yeye hakutawalishwa juu yao awalazimisha kuamini, na kwamba mwenye kugeuka na akakufuru baada ya waadhi huu ni Mwenyezi Mungu ndiye atakaye mshika kwa dhambi zake, na atamuadhibu kwa adhabu kubwa kabisa, atapo rejea kwake baada ya kufa, kwani marejeo ya wote na kuhisabiwa kwao wote ni kwake Yeye Mwenyezi Mungu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza?¹
2. Siku hiyo nyuso zitainama,²
3. Zikifanya kazi, nazo taabani.³
4. Ziingie katika Moto unao waka -⁴
5. Zikinyweshwa kutoka chemchem inayo chemka.⁵
6. Hawatakuwa na chakula isipo kuwa kichungu chenye miba.⁶
7. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.⁷
8. Siku hiyo nyuso nyengine zitakuwa kunjufu.⁸
9. Zitakuwa radhi kwa juhudi yao,⁹
10. Katika Bustani ya juu.¹⁰
11. Hawatasikia humo upuuzi.¹¹

1 Je! Ewe Muhammad! Imepata kukujiia hadithi ya Kiyama ambacho kwa vitisho vyake kitawafanya watu wazimie?

2 Siku hiyo ya Kiyama zitakuwepo nyuso zimedhalilika, zimechoka, taabani kwa shughuli na mashaka ya Motoni,

3 Tazama tanbihi ya 2.

4 Zinaingia kwenye Moto unao waka kwa nguvu!

5 Wananyweshwa maji yanayo toka kwenye chemchem inayo tokota

6 Hawana chakula ila chakula kiovu kabisa, anaadhibika mwenye kukila.

7 Hakileti nafuu yoyote katika mwili, wala hakiondoi njaa.

8 Na pia zitakuwepo nyuso zenye kutoa nuru Siku ya Kiyama, kwa malipo ya vitendo vyao walivyo fanya duniani. Hao watakuwa wameridhia kwa watayo yapata katika Pepo iliyo juu kwa pahala na cheo.

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Tazama tanbihi ya 8.

11 Humo halisikilizani neno la upuuzi. Humo mna chemchem isiyo katika.

12. Humo imo chemchem inayo miminika.¹²
13. Humo vimo viti vilivyo nyanyuliwa,¹³
14. Na bilauri zilizo pangwa,¹⁴
15. Na matakia safu safu,¹⁵
16. Na mazulia yaliyo tandikwa.¹⁶
17. Je! Hawamtazami ngamia jinsi alivyo umbwa?¹⁷
18. Na mbingu jinsi ilivyo inuliwa?¹⁸
19. Na milima jinsi ilivyo thibitishwa?¹⁹
20. Na ardhi jinsi ilivyo tandazwa?²⁰
21. Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji.²¹
22. Wewe si mwenye kuwatawalia.²²
23. Lakini anaye rudi nyuma na kukataa,²³
24. Basi Mwenyezi Mungu atamuadhibu kwa adhabu iliyo kubwa kabisa!²⁴
25. Hakika ni kwetu Sisi ndio marejeo yao.²⁵
26. Kisha hakika ni juu yetu Sisi hisabu yao!²⁶

12 Tazama tanbihi ya 11.

13 Humo vitakuwamo viti vilivyo nyanyuliwa kwa cheo na kwa hakika, kama ni ziada ya neema.

14 Na bilauri (gilasi) zilizo wekwa mbele yao.

15 Na mito na matakia yalio pangwa kwa safu.

16 Na mazulia mengi yaliyo tandazwa hapo barazani.

17 Je! Wanapuza kuzingatia Ishara, basi hebu na wamuangalie ngamia, vipi alivyo umbwa kwa namna ya peke yake kwa uweza wa Mwenyezi Mungu? (*Tazama Maelezo 88:17*)

18 Na waizingatie mbingu wanayo iona daima, vipi ilivyo nyanyuliwa huko mbali bila ya nguzo!

19 Na milima wanayo ikwea mpaka wakafika vileleni kwake, vipi ilivyo simamishwa kwa urefu, imeshikamana na ardhi, haiyumbi wala haitikisiki! (*Tazama Maelezo 88:19*)

20 Na ardhi wanayo ikalia na kuyendea juu yake, vipi ilivyo kunjuliwa na kutandazwa!

21 Basi kumbusha kwa wito wako, kwani kazi yako muhimu ni kufikisha wito tu. Hukuwa mtawala juu yao.

22 Tazama tanbihi ya 21.

23 Lakini miongoni mwao ataye puuza na akakataa, basi Mwenyezi Mungu atampa adhabu iliyo kubwa kabisa, isiyo kuwa na ya kuipita.

24 Tazama tanbihi ya 23.

25 Hakika ni kwetu Sisi marejeo yao kwa kifo na kufufuliwa, wala hapana penginepo isipo kuwa kwetu.

26 Tena ni juu yetu Sisi tu peke yetu kuwahisabia na kuwalipa.

Sura 89 - Al-Fajr

Utangulizi

Imeanza Sura hii kwa viapo vya mambo yanayo onekana namna mbali mbali, yanayo pelekea kuangalia athari ya kudra kwamba wanao mkanya Mwenyezi Mungu na kukanya kufufuliwa watakuja adhibiwa, kama walivyo kwisha adhibiwa walio kadhisha kabla yao. Na Sura ikaingia kuthibitisha mwendo wa Mwenyezi Mungu wa kuwajaribu waja wake kwa kheri na shari, na kwamba kupa kwake na kunyima kwake sio dalili ya kuridhika kwake au kukasirika kwake. Tena mazungumzo yakawaelekea wanao semezwa ya kwamba hali zao zinafichua wingi wa pupa yao na choyo chao. Kisha inakhitimisha kwa kuashiria majuto ya wanao pindukia kiasi na kutamani kwao kwamba laiti wangeli tanguliza mema ya kuwaokoa na hayo wanayo teseka nayo ya vitisho vya Siku ya Kiyama, na yanayo kuwa ya kuiliwaza nafsi iliyo tua iliyo tanguliza mema wala isikiuke mipaka, na itavyo itwa iingie pamoja na walio kirimiwa miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu katika Pepo ya Mwenyezi Mungu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa alfajiri,¹
2. Na kwa masiku kumi,²
3. Na kwa viwili viwili na kimoja kimoja,³
4. Na kwa usiku unapo pita,⁴
5. Je! Hapana katika haya kiapo kwa mwenye akili?⁵
6. Kwani hukuona jinsi Mola wako Mlezi alivyo wafanya kina A'di?⁶
7. Wa Iram, wenye majumba marefu?⁷
8. Ambao haukuumbwa mfano wake katika nchi?⁸
9. Na Thamudi walio chonga majabali huko bondeni?⁹
10. Na Firauni mwenye vigingi?¹⁰
11. Ambao walifanya jeuri katika nchi?¹¹

1 Naapa kwa mwangaza wa asubuhi unapo ufukuza usiku.

2 Na kwa masiku kumi yaliyo tukuzwa na Mwenyezi Mungu. (Na hayo ni masiku kumi ya mwanzo wa Mwezi wa Alhaj, Mfungo Tatu).

3 Na *shafi* yaani hisabu inayo gawika kwa mbili, kama 4, 6, 8 n.k. na *witri*, yaani isiyu gawika kwa mbili, kama 1, 3, 5 n.k. katika kila kitu.

4 Na kwa usiku unapo pita kwa kwenda ulimwengu kwa namna ya ajabu.

5 Je! Katika vitu vilivyo tajwa vinavyo onekana kwa akili hapana kiapo cha kukinaisha?

6 Kwani hujui jinsi Mola wako Mlezi alivyo wateremshia adhabu yake kaumu ya Hud, watu wa Iram wenye majengo marefu?

7 Tazama tanbihi ya 6.

8 Ambayo haikupata kujengwa mfano wake kwa umadhubuti na ujenzi katika nchi.

9 Kwani hukujua jinsi Mola wako Mlezi alivyo teremsha adhabu yake kwa Thamudi, kaumu ya Saleh, walio chonga majabali kujengea nyumba zao huko bondeni?

10 Au kwani hukujua vipi Mola wako Mlezi alivyo wateremshia adhabu yake Firauni mwenye majeshi yaliyo upa nguvu ufalme wake kama vigingi vinavyo simamisha makhema?

11 Ambao walipita mipaka katika nchi?

12. Wakakithirisha humo ufisadi?¹²
13. Basi Mola wako Mlezi aliwapiga mjeledi wa adhabu.¹³
14. Hakika Mola wako Mlezi yupo kwenye mavizio anawavizia.¹⁴
15. Ama mtu anapo jaribiwa na Mola wake Mlezi, akamkirimu na akamneemesha, husema: Mola wangu Mlezi amenikirimu!¹⁵
16. Na ama anapo mjaribu akampunguzia riziki yake, husema: Mola wangu Mlezi amenitia unyonge!¹⁶
17. Sivyo hivyo! Bali nyinyi hamuwakirimu mayatima,¹⁷
18. Wala hamhimizani kulisha masikini;¹⁸
19. Na mnakula urithi kwa ulaji wa pupa,¹⁹
20. Na mnapenda mali pendo la kupita kiasi.²⁰
21. Sivyo hivyo! Itakapo vunjwa ardhi vipande vipande,²¹
22. Na akaja Mola wako Mlezi na Malaika safu safu,²²
23. Na ikaletwa Jahannamu siku hiyo, siku hiyo mtu atakumbuka! Lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?²³
24. Atasema: Laiti ningeli jitangulizia kwa uhai wangu!²⁴
25. Basi siku hiyo hataadhibu yeyote namna ya kuadhibu kwake.²⁵
26. Wala hatafunga yeyote kama kufunga kwake.²⁶
27. Ewe nafsi iliyo tua!²⁷
28. Rejea kwa Mola wako Mlezi umeridhika, na umemridhisha.²⁸
29. Basi ingia miongoni mwa waja wangu,²⁹
30. Na ingia katika Pepo yangu.³⁰

12 Na wakazidisha kufanya uharibifu kwa ukafiri na udhalimu?

13 Basi Mola wako Mlezi aliwateremshia adhabu kali ya kuwaunguza.

14 Hakika Mola wako Mlezi anaviangalia vitendo vya watu, na anawahisabia, na atakuja kuwalipa kwavyo.

15 Ama mtu akijaribiwa na Mola wake Mlezi na akamkirimu, na akamneemesha kwa mali na cheo na nguvu, basi husema kwa kughurika na hayo: Mola wangu Mlezi amenitukuza kwa kuwa ninastahiki haya!

16 Na pindi Mola wake Mlezi akimjaribu mtu kwa kumdihakisha riziki, basi hughafilika na hikima ya hayo na husema: Mola wangu Mlezi kanidhalilisha!

17 Wacheni mtindo huo! Mambo siyo hayo kama msemavyo; bali nyinyi hamumkirimu yatima;

18 Wala hamhimizani kuwalisha masikini;

19 Na mnakula mali ya urithi kwa pupa, hamchagui linalo faa na lisilo faa.

20 Na mnayapenda mali mno, yanayo kupelekeeni kupapatika katika kuyakusanya na ubakhili wa kuyatumia.

21 Wacheni vitendo hivyo! Kwani inakungojeeni siku itapo lazwa ardhi iwe sawa sawa,

22 Na aje Mola wako Mlezi kama anavyo stahiki kuja kwake *Subhanahu* na Malaika waje kwa safu safu;

23 Na siku hiyo iletwe Jahannamu, nyumba ya adhabu, siku hiyo yatapo tokea hayo mwanaadamu atakumbuka aliyoharibu - lakini wapi! Kukumbuka huko kumfae nini, na wakati umekwisha pita?

24 Atasema kwa majuto: Laiti ningeli jitangulizia katika dunia vitendo vyema vya kunifaa katika maisha ya Akhera!

25 Siku hiyo zitakuwa hali hizi, haadhibu mtu kama adhabu ya Mwenyezi Mungu, wala hafungi mtu kama afungavyo Yeye.

26 Tazama tanbihi ya 25.

27 Ewe nafsi uliye tulia juu ya Haki!

28 Rejea kwenye radhi ya Mola wako Mlezi nawe uradhi kwa neema ulio pewa, nawe umemridhisha kwa a'mali uliyo ikadimisha.

29 Basi ingia katika kundi la waja wangu walio wema!

30 Na ingia katika Pepo yangu, nyumba ya neema ya milele!

Sura 90 - Al-Balad

Utangulizi

Mwenyezi Mungu anaapa kwa mji mtakatifu wa Makka, mji wa kuzaliwa Muhammad s.a.w. na ndipo alipo kulia na akapapenda, na pia anaapa kwa mzazi na anacho kizaa, kwani kwa hao ndio jinsi inahifadhika na maamrisha yanabakia, na ya kwamba mtu ameumbwa kwa mashaka na shida na taabu. Tena anabainisha kwamba mtu anadanganyika kwa kudhani kuwa uweza wake haushindiki, na kwamba yeye ana mali mengi anayo yatumia kuridhisha matamano yake na pumbao lake. Kisha *Subhanahu* akazitaja neema alizo mneemesha mwanaadamu na kumsahilishia njia za uwongofu na za kupitia milimani, ili awe katika watu wa Peponi, watu wa mkono wa kulia, na aikimbie njia ya kumpelekea kuwa katika watu wa kushoto ambako itawatumbukiza Motoni na kufungiwa milango.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa Mji huu!¹
2. Nawe unaukaa Mji huu.²
3. Na naapa kwa mzazi na alichokizaa.³
4. Hakika tumemuumba mtu katika taabu.⁴
5. Ati anadhani hapana yeyote ataye muweza?⁵
6. Anasema: Nimeteketeza chungu ya mali.⁶
7. Ati anadhani ya kuwa hapana yeyote anaye mwona?⁷
8. Kwani hatukumpa macho mawili?⁸
9. Na ulimi, na midomo miwili?⁹
10. Na tukambainishia zote njia mbili?¹⁰
11. Lakini hakujitoma kwenye njia ya vikwazo vya milimani.¹¹
12. Na nini kitakujuvya ni nini njia ya vikwazo vya milimani?¹²

1 Naapa kiapo cha mkazo kwa mji wa Makka, mji mtakatifu;

2 Na wewe unaishi katika mji huu, unauzidisha utukufu wake na cheo chake.

3 Na naapa kwa mzazi na anacho kizaa, na kwa hao wawili ndio jinsi inahifadhika na maendeleo yanabakia.

4 Hakika Sisi tumemuumba mtu katika mashaka na taabu tangu mwanzo wake mpaka kumalizika mambo yake.

5 Je! Anadhani mtu aliye umbwa katika mashaka haya kuwa hapana awezae kumdhalilisha?

6 Anasema: Nimetumia katika kupambana na Muhammad s.a.w. na kuupinga wito wake mali mengi ukiyakusanya pamoja.

7 Ati anadhani kwamba mambo yake hayo yamefichikana, hayajui yeyote hata huyo aliye muumba?

8 Kwani Sisi hatukumuumba na macho mawili ya kutazamia, na ulimi na midomo miwili ili aweze kutamka na kusema sawa?

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Na tukamwonyesha njia ya kheri na ya shari, na tukamtengenezea aweze kuchagua mojawapo?

11 Basi huyo hakunafika kwa tuliyo mtengenezea, wala hakuivuka njia ya milimani inayo mzuia asifikie uwokovu, nayo ni choyo wa nafsi yake.

12 Na kitu gani kitakufunza nini huko kujitoma kwenye njia ya milimani?

13. Kumkomboa mtumwa;¹³
14. Au kumlisha siku ya njaa¹⁴
15. Yatima aliye jamaa,¹⁵
16. Au masikini aliye vumbini.¹⁶
17. Tena awe miongoni mwa walio amini na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana.¹⁷
18. Hao ndio watu wa kheri wa kuliani.¹⁸
19. Lakini walio zikataa Ishara zetu, hao ndio watu wa shari wa kushotoni.¹⁹
20. Juu yao utakuwa Moto ulio fungwa kila upande.²⁰

13 Kumkomboa mtu kutokana na utumwa,

14 Au kumlisha siku ya njaa.

15 Yatima aliye jamaa wa kumliwaza kwa ujamaa na ufakiri.

16 Au masikini mwingi wa haja na kufakirika.

17 Tena awe pamoja na hayo miongoni mwa wenye Imani wanao usiana na wenzao kwa subira na kuoneana huruma.

18 Hao wanao sifika kwa sifa hizi, ndio watu wa kheri, wa mkono wa kulia.

19 Na walio zikataa dalili tulizo zisimamisha kuthibitisha Haki kutoka na Kitabu na hoja zake, hao ndio wapotovu watu waovu walio kosa kheri na watapata adhabu.

20 Juu yao utakuwa Moto ulio bebeana na milango yake ikafungwa.

Sura 91 - Ash-Shams

Utangulizi

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa kuanzia Sura hii kwa vitu kadhaa wa kadhaa miongoni mwa viumbe vyake vitukufu, vyenye kueleza utimilivu wa uweza wake Mwenyezi Mungu Mtukufu na Upweke wake, juu ya kufuzu kwa mwenye kuisafisha nafsi yake kwa Imani na ut'iifu, na kukhasiri kwa kupinga mwenye kuidhoofisha kwa ukafiri na maasi. Kisha ikaingilia mfano wa Thamudi, kaumu ya Saleh, na yaliyo wafika hao, ili apate kuzingatia kila mwenye inda mwenye kukadhibisha. Kwani hakika wao walipo mkadhibisha Mtume wao, na wakamuwa yule ngamia, Mwenyezi Mungu aliwaangamiza wote, na Yeye hakhofu matokeo ya kuwaangamiza hao, na aliyo wateremshia, kwani Yeye hasailiwi kwa anayo yatenda, na hakika amewateremshia wanayo stahiki.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa jua na mwangaza wake!¹
2. Na kwa mwezi unapo lifuatia!²
3. Na kwa mchana unapo lidhihirisha!³
4. Na kwa usiku unapo lifunika!⁴
5. Na kwa mbingu na kwa aliye ijenga!⁵
6. Na kwa ardhi na kwa aliye itandaza!⁶
7. Na kwa nafsi na kwa aliye itengeneza!⁷
8. Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake,⁸
9. Hakika amefanikiwa aliye itakasa,⁹
10. Na hakika amekhasiri aliye iviza.¹⁰
11. Kina Thamudi walikadhibisha kwa sababu ya upotofu wao,¹¹
12. Alipo simama mwovu wao mkubwa,¹²
13. Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu alipo waambia: Huyu ni ngamia wa Mwenyezi

1 Naapa kwa jua na mwangaza wake na kuchomoza kwake na kwa joto lake!

2 Na kwa mwezi unapo lifuata na likawa nyuma yake kwa kutoa mwangaza baada ya kuchwa jua.

3 Na kwa mchana unapo lidhihirisha jua, likaonekana wazi halikufichikana.

4 Na kwa usiku unapo lifunika jua, ukawa mwangaza wake hauonekani.

5 Na kwa mbingu na kwa Mweza Mtukufu aliye inyanzua na akaijenga kwa hikima yake.

6 Na kwa ardhi na kwa Mweza Mtukufu aliye ikunjua kwa kila upande, na akaitengeneza kwa ajili ya utulivu, na akaifanya kama tandiko.

7 Na kwa nafsi, na aliye iumba na akaiweka sawa, kwa kuipa nguvu,

8 Akaifunza jema na baya, na akaipa uweza wa kutenda itakayo katika hayo.

9 Hakika amefuzu mwenye kuisafisha nafsi yake kwa ut'iifu na vitendo vya kheri.

10 Na hakika amekhasiri mwenye kuzificha fadhila zake, na akayaua matayarisho aliyo umbwa nayo ya kutenda kheri.

11 Kina Thamudi walimkanusha Nabii wao kwa upotovu wao na jeuri zao, alipo gutuka mwovu wao mkubwa kabisa kutaka kumchinja ngamia.

12 Tazama tanbihi ya 11.

Mungu, mwacheni anywe maji fungu lake.¹³

14. Lakini walimkadhibisha na wakamchinja ngamia, kwa hivyo Mola wao Mlezi aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na akawafuta kabisa.¹⁴

15. Wala Yeye haogopi matokeo yake.¹⁵

13 Saleh, Mtume wa Mwenyezi Mungu, akawaambia: Mwachilieni huyu ngamia wa Mwenyezi Mungu ale maridhawa katika ardhi ya Mwenyezi Mungu, na tahadharini msimzuie maji katika siku yake aliyo wekewa.

14 Wakamkadhibisha Mtume wao katika hilo onyo lake, wakamchinja. Mola wao Mlezi akazibomoa nyumba zao kwa sababu ya dhambi zao; akazisawazisha na ardhi!

15 Wala Yeye Mwenyezi Mungu hakhofu matokeo ya adhabu hiyo, kwani hiyo ni malipo ya haki kwa yale waliyo yatenda.

Sura 92 - Al-Layl

Utangulizi

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa kwa viapo vitatu juu ya kuwa vitendo vya watu vinakhitalifiana, baadhi yake ni vya uwongofu, na baadhi yake ni vya upotofu. Mwenye kutoa, na akamchamngu, na akawafiki tabia yenye kukusanya kheri, basi Mwenyezi Mungu atamsahilishia mambo yake kwa wepesi. Na mwenye kufanya ubakhili, na akajiona hana haja na mtu, na akakanusha tabia zenye kukusanya kheri Mwenyezi Mungu atamfanyia wepesi kuingia mashakani. Na wala mali yake hayatamfaa kitu kumwoko akitumbukia katika adhabu! Na Aya zikabainisha baada ya hayo kwamba hakika Mwenyezi Mungu amechukua jukumu kubainisha njia za uwongofu kwa fadhila zake, na kwake yapo mambo ya maisha mawili, ya Akhera na ya duniani. Na kwamba hakika Yeye amekwisha onya kwamba Moto watauingia waovu na watauepuka walio wema.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa usiku unapo funika!¹
2. Na mchana unapo dhihiri!²
3. Na kwa Aliye umba dume na jike!³
4. Hakika juhudi zenu bila ya shaka ni mbali mbali.⁴
5. Ama mwenye kutoa na akamchamngu,⁵
6. Na akaliwafiki lilio jema,⁶
7. Tutamsahilishia yawe mepesi.⁷
8. Na ama mwenye kufanya ubakhili, na asiwe na haja ya wenzake,⁸
9. Na akakanusha lilio jema,⁹
10. Tutamsahilishia yawe mazito!¹⁰
11. Na mali yake yatamfaa nini atapo kuwa anadidimia?¹¹

1 Naapa kwa usiku kinapo enea kiza chake!

2 Na naapa kwa mchana unapo zagaa mwangaza wake!

3 Na naapa kwa Mjuzi aliye umba viwili viwili, dume na jike, katika kila vinavyo zaliwa!

4 Hakika juhudi zenu bila ya shaka zimekhitalifiana; kwani wapo wenye kubahatika katika juhudi zao, na wako wasio bahatika.

5 Ama mwenye kutoa katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na akamkhofu Mola wake Mlezi, na kwa hivyo akaepuka anayo yakataza, na akayakinika kufuata fadhila njema, nayo ni Imani kumuamini Mwenyezi Mungu kwa kumjua, basi Sisi tutamtengenezea awe katika khulka ya wepesi na raha kwa kumwongoza kwenye njia ya kheri.

6 Tazama tanbihi ya 5.

7 Tazama tanbihi ya 5.

8 Ama mwenye kufanya ubakhili kwa mali yake asitoe haki ya Mwenyezi Mungu iliomo humo, na akawa hana haja na yatokayo kwa Mwenyezi Mungu, na akakadhibisha khulka nzuri, basi huyo tutamtengenezea khulka ambayo inapelekea uzito na mashaka ya milele.

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Tazama tanbihi ya 8.

11 Na kitu gani katika adhabu ambacho hayo mali yake yataweza kumkinga nacho, atapo teketea yeye

12. Hakika ni juu yetu kuonyesha uwongofu.¹²
13. Na hakika ni yetu Sisi Akhera na dunia.¹³
14. Basi nakuonyeni na Moto unao waka!¹⁴
15. Hatauingia ila mwovu kabisa!¹⁵
16. Anaye kadhhibisha na kupa mgongo.¹⁶
17. Na mchamngu ataepushwa nao,¹⁷
18. Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa.¹⁸
19. Na wala si kwa kuwa yupo yeyote aliye mfanyia hisani ndio anamlipa.¹⁹
20. Ila ni kutaka radhi ya Mola wake Mlezi aliye juu kabisa.²⁰
21. Naye atakuja ridhika!²¹

mwenyewe mzima?

12 Hakika ni juu yetu, Sisi, kwa kufuatana na hikima yetu, ndio tuwabainishie viumbe njia ya uwongofu.

13 Na juu yetu Sisi peke yetu, bila ya shaka, hili jambo la kuendesha yaliomo duniani na Akhera.

14 Ndio maana tukakutieni khofu ya Moto unao waka na kuripuka!

15 Hawauingii kwa kudumu ila kafiri aliye ikadhhibisha Haki na akazipuuza Ishara za Mola wake Mlezi.

16 Tazama tanbihi ya 15.

17 Na atakuwa mbali na huo Moto aliye mwingi wa kujikinga na ukafiri na maasi, amabye hutoa mali yake wakati wa nafasi ili kujisafisha na uchafu wa ubakhili, na najsi ya uchoyo.

18 Tazama tanbihi ya 17.

19 Na mtoaji huyu si kama anaye mtu yeyote ambaye ndio anamlipa kwa neema aliyo mfanyia zamani,

20 Bali anatoa hicho kwa kutafuta radhi ya Mola wake Mlezi Mtukufu tu.

21 Na bila ya shaka atakuja pata kutoka kwa Mola wake Mlezi anacho kitaka kwa njia za ukamilifu kabisa, hata itimie radhi kwake.

Sura 93 - Adh-Dhuh'aa

Utangulizi

Sura hii imeanza kwa viapo viwili vyenye kueleza nyakati mbili za uchangamfu na za kutulia, ya kwamba kwa hakika Mwenyezi Mungu hakumwacha Mtume wake wala hakumchukia, na kwamba aliyo mtengenezea katika Akhera makao ya juu ni bora zaidi kuliko alio mkirimu duniani. Kisha *Subhanahu* akaapa kwamba Yeye atampa mpaka aridhike, na yaliyo tangulia ni ushahidi wa yatakayo kuja. Kwani alikuwa yatima, akampatia makaazi; alikuwa amepotea akampa bora ya uwongofu, na alikuwa fakiri akamtajirisha. Kisha Aya zikataka aangaliwe vyema yatima, na asikemewe mwenye kuomba au kuuliza, na zisimuliwe neema za Mwenyezi Mungu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa mchana!¹
2. Na kwa usiku unapo tanda!²
3. Mola wako Mlezi hakukuacha, wala hakukasirika nawe.³
4. Na bila ya shaka wakati ujao utakuwa bora kwako kuliko ulio tangulia.⁴
5. Na Mola wako Mlezi atakupaa mpaka uridhike.⁵
6. Kwani hakukukuta yatima akakupaa makaazi?⁶
7. Na akakukuta umepotea akakuongoa?⁷
8. Akakukuta mhitaji akakutosheleza?⁸
9. Basi yatima usimwonee!⁹
10. Na anaye omba au kuuliza usimkaripie!¹⁰
11. Na neema za Mola wako Mlezi zisimlie. ¹¹

1 Naapa kwa wakati wa kupanda juu jua, na ni wakati wa uchangamfu na kazi!

2 Na naapa kwa usiku unapo tulia na ukatanda kote kiza chake!

3 Ewe Muhammad! Mola wako Mlezi hakukuacha, wala hakukuchukia.

4 Na matokeo ya mambo yako, mwisho wake, yatakuwa bora kuliko mwanzo wake.

5 Na ninaapa kuwa bila ya shaka hapo Mola wako Mlezi atakupaa kheri za duniani na Akhera hata utaridhia.

6 Kwani hakukukuta wewe yatima unahitaji wa kukutunza naye akakupaa makaazi ya kukuhifadhi kwa mwenye kukuangalia vyema kwa mambo yako?

7 Na akakuona umebabaika hukukinaika na itikadi zilizo kuzunguka, naye akakuongoa kwenye Njia ya Haki?

8 Akakukuta fakiri wa mali naye akakutajirisha kwa kukupaa riziki?

9 Ikiwa hii ndiyo hali yetu nawe, basi yatima usimdhili, na mwenye kuomba au kuuliza usimjibu kwa ukavu, na ama neema za Mola wako Mlezi zitangaze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuwa ndio kudhihirisha neema.

10 Tazama tanbihi ya 9.

11 Tazama tanbihi ya 9.

Sura 94 - Ash-Sharh'

Utangulizi

Inathibitisha Sura hii kwamba Mwenyezi Mungu ameukunjua moyo wa Nabii wake, na akaufanya ndipo pahala pa kuteremkia siri na ilimu, na akaondoa matatizo yaliyo kuwa yakimthakilisha mgongo wake, nayo ni katika mizigo ya kazi ya Da'wa, yaani Wito. Na akalikutanisha jina lake Mwenyezi Mungu na jina lake Mtume katika asli ya Imani na alama za Dini. Kisha Aya hizi zikataja sunna ya Mwenyezi Mungu ya kuambatisha mepesi na mazito, dhiki na faraji, na zikamtaka Mtume kila anapo pata nafasi kutokana na kutenda kheri, atende kheri nyengine, na afanye lengo lake ni Mola wake Mlezi, kwani Yeye ni Muweza wa kumsaidia.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Hatukukunjulia kifua chako?¹
2. Na tukakuondolea mzigo wako,²
3. Ulio vunja mgongo wako?³
4. Na tukakunyanyulia utajo wako?⁴
5. Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi,⁵
6. Hakika pamoja na uzito upo wepesi.⁶
7. Na ukipata faragha, fanya juhudi.⁷
8. Na Mola wako Mlezi ndio mshughulikie.⁸

1 Hakika tumekukunjulia kifua chako kwa kuwa tulitia ndani yake Uwongofu na Imani.

2 Na tumekupunguzia mizigo iliyo kuwa mizito juu ya mgongo wako, kwa kukuunga mkono na kukusahilishia mambo yako,

3 Ambayo yalikuwa ni mazito juu ya mgongo wako.

4 Na tumelitukuza jina lako, tukalifanya linatajwa na ulimi wa kila Muumini pamoja na jina letu.

5 Hizo ni baadhi ya neema zetu juu yako. Basi kuwa na yakini na uweza wa Mwenyezi Mtukufu, kwani pamoja na uzito upo wepesi mwingi unao kuja nao.

6 Hakika pamoja na uzito (wakati huo huo ijapo kuwa wewe hujui), upo wepesi mwingi vile vile.

7 Basi ukipata nafasi katika kazi ya kuwalingania watu, na mambo yaliyo khusiana na Jihadi, endelea na jitihada ya ibada na jishughulisha nafsi yako katika hayo.

8 Kwa Mola wako Mlezi tu ndio uelekee kwa kumwomba na kumhitajia.

Sura 95 - At-Tin

Utangulizi

Mwenyezi Mungu anaapa katika Sura hii kwa matunda mawili yenye baraka, na pahala pawili pazuri, ya kwamba Yeye hakika amemuumba mtu kwa njia kunjufu kabisa, kwa kumkamilishia akili, na uwezo wa kutaka na kutotaka, na mengineyo katika sifa za ukamilifu. Kisha Aya zikataja kuwa mtu hakusimama kwa mujibu wa alivyo umbiwa, bali akateremka kwa daraja mpaka akawa wa chini kabisa, isipo kuwa walio amini na wakatenda mema kati yao. Hao Mwenyezi Mungu amewakunjulia vipawa. Kisha Sura imewageukia kuwakemea wanao kadhibisha kufufuliwa baada ya kudhihiri dalili zote za uweza wa Mwenyezi Mungu na khabari za hikima yake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa tini na zaituni!¹
2. Na kwa Mlima wa Sinai!²
3. Na kwa mji huu wenye amani!³
4. Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa.⁴
5. Kisha tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini!⁵
6. Lakini wale walio amini na wakatenda mema, hao watapata ujira usio kwisha.⁶
7. Basi ni kipi baadaye kitacho kukukadhibishia malipo?⁷
8. Kwani Mwenyezi Mungu si muadilifu kuliko mahakimu wote?⁸

1 Naapa kwa tini na zaituni, kwa baraka zao na ubora wa manufaa yao.

2 Na kwa mlima ambao juu yake ndio Mwenyezi Mungu alimsemeza Musa.

3 Na kwa huu mji mtukufu wa Makka, ambao anaushuhudia utukufu wake mwenye kwenda uzuru, na anapata amani mwenye kuuingia.

4 Kwa hakika bila ya shaka yoyote Sisi tumemuumba mtu amesimama sawa kwa umbo bora kabisa lilio nyooka, na akasifika kwa sifa nzuri kabisa.

5 Kisha tukamteremsha cheo mpaka akawa ni wa chini kabisa katika hao walioko chini, kwa kuacha kufanya waajibu wa hayo tuliyo muumbia.

6 Lakini walio amini na wakatenda vitendo vyema, hao basi watapata ujira usio wakatikia wala kuwapungukia.

7 Basi kitu gani kinacho kupelekea kukadhibisha kufufuliwa na kulipwa baada ya kuwekwa wazi uweza wetu wa hayo?

8 Kwani Mwenyezi Mungu aliye yatenda hayo tuliyo kueleza si muadilifu kuliko mahakimu wote kwa kufanya na kupanga?

Sura 96 - Al-'Alaq

Utangulizi

Katika Sura hii upo wito wa kusoma na kujifunza, na kwamba aliye weza kumuumba mtu kutokana na asli nyonge ni Muweza wa kumfunza kuandika kwa kudhibitia ilimu na kutimizia kufahamu, na amfunze aliyo kuwa hayajui. Kwani Yeye *Subhanahu* ndiye Mwenye kummiminia ilimu mwanaadamu. Na Sura inabihisha kwamba utajiri na nguvu huenda zikampelekea mtu kupindukia mipaka ya Mwenyezi Mungu, lakini marejeo ya wote ni kwa Mwenyezi Mungu mwishoni. Na mazungumzo yanamwelekea kila mwenye kusilihi kusemezwa kuwaonya hao majeuji wanao pinga kheri, kuwaonya kuwa watakuja kushikwa kwa nywele zao za utosi wakibururwa Motoni; na hawatofaliwa na wasaidizi wowote. Na Sura inakhitimisha kwa kuwataka wasikivu wende kinyume na hao wenye inda wanao kadhibisha, na wajijongeze kwa ut'iifu kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Soma kwa jina la Mola wako Mlezi aliye umba,¹
2. Amemuumba binaadamu kwa tone la damu,²
3. Soma! Na Mola wako Mlezi ni Karimu kushinda wote!³
4. Ambaye amefundisha kwa kalamu.⁴
5. Kamfundisha mtu aliyo kuwa hayajui.⁵
6. Kwani! Hakika mtu bila ya shaka huwa jeuri⁶
7. Akijiona katajirika.⁷
8. Hakika kwa Mola wako Mlezi ndio marejeo.⁸
9. Umemwona yule anaye mkataza⁹
10. Mja anapo sali?¹⁰
11. Umeona kama yeye yuko juu ya uwongofu?¹¹

1 Ewe Muhammad! Soma unayo funuliwa kwa kufunguliwa kwa Jina la Mola wako Mlezi ambaye ni Yeye tu peke yake ndiye Mwenye uweza wa kuumba.

2 Amemuumba mtu kwa ukamilifu wa mwili wake na ilimu kutokana na kipande cha damu ambacho hakina chochote cha kupelekea kujiona bora.

3 Endelea na kusoma, na Mola wako Mlezi aliye Karimu kushinda wote, atakutukuza wala hatakuharau.

4 Yeye ndiye ambaye aliye mfunza mtu kuandika kwa kalamu, na wala kwanza hakuwa anajua hayo.

5 Amemfunza mtu yasiyo kuwa yanampitia katika mawazo yake.

6 Ni hakika kweli mtu hupindukia mpaka na hupanda kiburi mbele ya Mola wake Mlezi anapo jiona si mhitaji, katajirika.

7 Tazama tanbihi ya 6.

8 Ewe Muhammad! Hakika ni kwa Mola wako Mlezi peke yake ndiyo yako marejeo ya wote kwa kufufuliwa na kulipwa.

9 Je! Umemwona huyu jeuri anaye mzuia mja asisali anapo taka kusali?

10 Tazama tanbihi ya 9.

11 Hebu niambie khabari za jeuri huyu kama yeye yumo katika uwongofu katika huku kuzuia kwake, au kwamba ndio anaamrisha uchamngu katika hayo anayo amrisha!

12. Au anaamrisha uchamngu?¹²
13. Umeona kama yeye akikanusha na anarudi nyuma?¹³
14. Hajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anaona?¹⁴
15. Kwani! Kama haachi, tutamkokota kwa shungi la nywele!¹⁵
16. Shungi la uwongo, lenye makosa!¹⁶
17. Basi na awaite wenzake!¹⁷
18. Nasi tutawaita Mazabania!¹⁸
19. Hasha! Usimt'ii! Nawe sujudu na ujongee!¹⁹

12 Tazama tanbihi ya 11.

13 Niambie khabari za huyu mwenye kukataza anapo yakadhibisha aliyo kuja nayo Mtume, na akapuuza Imani na vitendo vyema.

14 Hivyo hajui kwamba Mwenyezi Mungu anazijua vyema hali zake, naye atamlipa kwazo?

15 Kwa kumkemea huyu mwenye kuzuia, anaambiwa kama hakuacha hayo anayo yafanya, basi hapana shaka tutamkokota kwa nguvu tukimshika kwa shungi lake la nywele mpaka Motoni!

16 Hilo shungi lilio juu ya uso wake mwenye kuropokwa uwongo na mwenye athari za ukosefu!

17 Basi yeye awaite wenziwe na watu wa baraza lake wawe ndio wasaidizi duniani au Akhera.

18 Sisi tutawaita askari wetu wamsaidie Muhammad na walio pamoja naye, na wapambane na huyo mwenye kukanya na wasaidizi wawasukume kwenye Jahannamu

19 Kumnyamazisha huyu mwenye kuzuia, wewe usimkubalie kwa hayo anayo kukataza nayo, na dumu juu ya Sala zako, na endelea na sijida zako, na jijongee kwa Mola wako Mlezi kwa hivyo.

Sura 97 - Al-Qadr

Utangulizi

Katika Sura hii inasifiwa shani ya Qur'ani na shani ya Usiku ilipo teremshwa Qur'ani, na inaelezwa kwamba usiku huo mmoja ni bora kuliko miezi elfu, na kwamba hakika Malaika na Jibrili huteremka usiku huo kwa idhini ya Mola wao Mlezi kwa ajili ya kila amri, kwa kusalimika na kila maudhi na uovu mpaka kuchomoza alfajiri yake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Hakika Sisi tumeiteremsha Qur'ani katika *Laylatul Qadri*, Usiku wa Cheo Kitukufu.¹
2. Na nini kitacho kujuulisha nini *Laylatul Qadri*?²
3. *Laylatul Qadri* ni bora kuliko miezi elfu.³
4. Huteremka Malaika na Roho katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao Mlezi kwa kila jambo.⁴
5. Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri.⁵

1 Hakika Sisi tumeiteremsha Qur'ani katika usiku wa Cheo na Utukufu.

2 Na kitu gani kitakufunza ni nini usiku huo wa Cheo na Utukufu?

3 Usiku wa Qadr na Sharaf, Cheo na Utukufu, ni bora kuliko miezi elfu, kwa kuwa umekhusika kwa kuteremka ndani yake Qur'ani tukufu.

4 Huteremka Malaika na Jibrili katika usiku huo mpaka kwenye ardhi kwa idhini ya Mola wao Mlezi kwa sababu ya kila jambo.

5 Na wameaminika na maudhi na uovu. Hali inabaki hivyo mpaka mapambazuko ya alfajiri.

Sura 98 - Al-Bayyinah

Utangulizi

Watu wa Kitabu, yaani Mayahudi na Wakristo, wamejua kutokana na Vitabu vyao, na washirikina wa Makka wakajua kutokana nao sifa za Nabii wa zama za mwisho. Na yalikuwa yanatakikana kutokana na hayo ni kuwa wamuamini huyo Nabii pindi akiteuliwa. Lakini alipo teuliwa miongoni mwao Mtume wa Mwenyezi Mungu mwenye kuungwa mkono na Qur'ani, walikhitalifiana na wakaacha ahadi yao. Na vitendo vya Watu wa Kitabu katika hayo vilikuwa viovu zaidi kuliko vya washirikina. Na hukumu ya watu hawa wote Akhera ni kukaa milele katika Moto. Na Waumini, watu wa vyeo vya juu kwa fadhila, ndio bora wa viumbe. Malipo yao ni kukaa milele Peponi, na kuridhika kwa kuyapata wayatakayo na kupewa wanayo yapenda. Hii ndiyo neema ya mwenye kumkhofu Mola wake Mlezi.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Hawakuwa walio kufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu na washirikina waache walio nayo mpaka iwajie bayana,¹
2. Yaani Mtume aliye toka kwa Mwenyezi Mungu anaye wasomea kurasa zilizo takasika,²
3. Ndani yake mna maandiko yaliyo nyooka.³
4. Wala hawakufarikiana walio pewa Kitabu ila baada ya kuwajia hiyo bayana.⁴
5. Nao hawakuamrisha kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na washike Sala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini madhubuti.⁵
6. Hakika walio kufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu na washirikina wataingia katika Moto wa Jahannamu wadumu milele humo. Hao ndio viumbe waovu kabisa.⁶

1 Hawakuwa walio mkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake miongoni mwa Mayahudi na Wakristo, na miongoni mwa washirikina, waache kughafilika kwao na ujinga wao kuto ijua Haki mpaka iwajie hoja ya kukata.

2 Na hoja hiyo ni Mtume aliye tumwa kutokana na Mwenyezi Mungu awasomee kurasa zilizo takasika na upotovu, ndani yake zimo hukumu zilizo sawa zenye kutamka kwa haki na kwa yaliyo ndiyo.

3 Tazama tanbihi ya 2.

4 Wala hawakufarikiana walio pewa Kitabu katika Mayahudi na Wakristo, ila baada ya kuwajia hiyo hoja iliyo wazi yenye kuonyesha ya kwamba Muhammad ndiye huyo Mtume wa Mwenyezi Mungu aliye ahidiwa katika Vitabu vyao.

5 Na hawakulazimishwa jambo katika walio lazimishwa ila iwe ibada yao kwa Mwenyezi Mungu na kumsafia Yeye Dini, waache upotovu wasimame sawa kwenye Haki, na wazihifadhi Sala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Mila Iliyo Nyooka.

6 Hakika wale walio kufuru katika Watu wa Kitabu na washirikina wataingia katika Moto wa Jahannamu,

7. Hakika walio amini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe.⁷

8. Malipo yao kwa Mola wao Mlezi ni Bustani za daima, zipitazo mito kati yake. Wakae humo milele. Mwenyezi Mungu yu radhi nao, na wao waradhi naye. Hayo ni kwa anaye mwogopa Mola wake Mlezi.⁸

wala hawatatoka humo. Hao ndio waovu wa viumbe kwa itikadi na vitendo.

7 Hakika wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakatenda vitendo vyema, hao ndio bora ya viumbe kwa itikadi na vitendo.

8 Malipo yao Akhera kwa Imani na vitendo vyema walivyo vitanguliza, ni Mabustani ya kudumu yenye kupitiwa na mito kati yake, watakaa humo milele. Mwenyezi Mungu amepokea a'mali zao, na wao watamshukuru kwa hisani yake aliyo wafanyia. Hiyo ndiyo jaza ya mwenye kuiogopa adhabu ya Mola wake Mlezi, akaamini na akatenda mema.

Sura 99 - Az-Zilzalah

Utangulizi

Aya za Sura hii zote hazipindikii hali za Kiyama:-

Mtikisiko wa ardhi, na kutoka khazina na maiti walio zikwa chini, na kustaaajabu kwa binaadamu na kuuliza kwake kwa yale yaliyo mkumba kwa ghafla, na kutoka watu makaburini mwao kwa mtafaruku wende kupokea malipo yao!

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Itakapo tetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wake!¹
2. Na itakapo toa ardhi mizigo yake!²
3. Na mtu akasema: Ina nini?³
4. Siku hiyo itahadithia khabari zake.⁴
5. Kwa sababu Mola wake Mlezi ameifunulia!⁵
6. Siku hiyo watu watatoka kwa mfarakano wakaonyweshwe vitendo vyao!⁶
7. Basi anaye tenda chembe ya wema, atauona!⁷
8. Na anaye tenda chembe ya uovu atauona!⁸

1 Ikitisika ardhi kwa mtikiso mkubwa, na ikasukika kwa ukomo wa kutisika na kusukika kunako mkinika na ikaweza kuchukua!

2 Na ardhi ikatoa yote yaliomo katika ndani ya tumbo lake, ikiwa khazina au maiti walio kwisha zikwa!

3 Na binaadamu akasema kwa kushtuka na khofu: Ardhi hii ina nini hata inatikisika hivi, na inatoa vilivyomo tumboni mwake, ndio Saa imefika?

4 Siku hiyo ardhi itamsimulia mtu khabari zake zilizo mshitua, kwani Mlezi wake na Muumba wake atakuwa kaifunulia, kaipa Wahyi, na kaiaamuru itetemeke na ijisuke suke, ndio ikafanya upesi kutekeleza amri.

5 Tazama tanbihi ya 4.

6 Siku hiyo watu watatoka makaburini mbio, nao wamo katika mtafaruku, wapate kuziona hisabu zao na malipo yao aliyo waahidi Mwenyezi Mungu.

7 Basi mwenye kufanya hata kitu chenye uzito wa punje ya mchanga cha kheri ataiona katika daftari lake, na atapata malipo yake.

8 Na mwenye kufanya shari ya uzito wa chembe ya mchanga ataiona kadhaalika, na atapata malipo yake. Wala Mola wako Mlezi hatamdhulumu yeyote.

Sura 100 - Al-'Aadiyaat

Utangulizi

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa katika kifungulio cha Sura hii kwa farasi wa Jihadi, kwamba hakika mwanaadamu bila ya shaka ni mwingi wa kuikufuru neema ya Mola wake Mlezi. Na kwamba juu ya hivyo katika Akhera bila ya shaka atakuwa ni shahidi dhidi ya nafsi yake kwa aliyo kuwa nayo. Na kwamba bila ya shaka yeye kwa kuyapenda mali ni bakhili na mwenye choyo juu yake. Na khatimaye ametaja khabari za kufufuliwa, na akazindua kuwa ipo hisabu na malipo.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa farasi wendao mbio wakipumua,¹
2. Na wakitoa moto kwa kupiga kwato zao chini,²
3. Wakishambulia wakati wa asubuhi,³
4. Huku wakitimua vumbi,⁴
5. Na wakijitoma kati ya kundi,⁵
6. Hakika mwanaadamu ni mtovu wa fadhila kwa Mola wake Mlezi!⁶
7. Na hakika yeye mwenyewe bila ya shaka ni shahidi wa hayo!⁷
8. Naye hakika bila ya shaka ana nguvu za kupenda mali!⁸
9. Kwani hajui watakapo fufuliwa waliomo makaburini?⁹
10. Na yakakusanywa yaliomo vifuani?¹⁰
11. Kuwa hakika Mola wao Mlezi siku hiyo bila ya shaka atakuwa na khabari zao wote!¹¹

1 Ninaapa kwa farasi wa Jihadi wendao mbio, na huku pumzi zao zinasikilizana kwa sauti inayo itwa "Dh'abh'an".

2 Na kwa farasi hao ambao hutoa cheche za moto zinapo gonga kwato zao kwenye ardhi wanapo kwenda.

3 Na kwa farasi hao wanao washambulia maadui asubuhi kabla jua halijachomoza;

4 Wakatimua mavumbi mengi, farasi hao, kati ya makundi ya maadui!

5 Ikawa vumbi limewagubika maadui hata wakaingiwa kiwewe na kufazaika.

6 Hakika mwanaadamu ni mwingi wa kuzikufuru neema za Mola wake Mlezi ambazo hazikadiriki.

7 Na hakika yeye mwenyewe bila ya shaka atakuwa mwingi wa kuja jishuhudia huko Akhera kwa kuungama madhambi yake.

8 Na hakika yeye kwa uchoyo na kuyapenda mali alio nayo, ni bakhili, hatoi kama inavyo mwajibikia katika mali yake.

9 Kwani hajui mwisho wa hali yake, hata hajui wakitolewa maiti waliomo makaburini, na vikakusanywa viliomo vifuani navyo vimekwisha sajiliwa katika madaftari yao, yakiwa mema au mabaya waliyo yatenda.

10 Tazama tanbihi ya 9.

11 Kwamba hakika Mlezi wao na Muumba wao bila ya shaka anajua vyema vitendo vyao na malipo yao Siku ya Kufufuliwa na Kulipwa.

Sura 101 - Al-Qaari'ah

Utangulizi

Sura hii inaanza kwa kitisho cha hiyo *AL-QAARIA'H*, yaani Inayo gonga, sauti inayo gonga katika masikio ya watu, yaani ndio Kiyama. Na Sura imetaja baadhi ya hali za hiyo sauti inayo gonga khasa kwa mintarafu ya watu na milima. Na ikashughulikia kusimulia hao ambao mizani yao itakuwa nzito kwa kuzidi mema yao, na mizani yao itayo kuwa duni kwa kuzidi maovu yao (na kupunguka mema yao).

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Inayo gonga!¹
2. Nini Inayo gonga?²
3. Na nini kitacho kujulisha nini Inayo gonga?³
4. Siku ambayo watu watakuwa kama nondo walio tawanyika;⁴
5. Na milima itakuwa kama sufi zilizo chambuliwa!⁵
6. Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito,⁶
7. Huyo atakuwa katika maisha ya kupendeza.⁷
8. Na yule ambaye mizani yake itakuwa khafifu,⁸
9. Huyo maskani yake yatakuwa Moto wa Hawiya!⁹
10. Na nini kitacho kujulisha nini hiyo?¹⁰
11. Ni Moto mkali!¹¹

1 *AL-QAARIA'H*, Inayo gonga, ni Kiyama, ambacho kinaanza kwa mpulizo wa mwanzo wa barugumu, na kinaishia itapo katwa hukumu baina ya watu.

2 Kitu gani kilicho cha ajabu zaidi katika ukuu wake, na khatari zake na kitisho chake!

3 Na kitu gani kitacho kujulisha hali ya *AL-QAARIA'H* katika kitisho chake juu ya nafsi za watu?

4 Siku hiyo watu watakuwa kama vipepeo kwa wingi na kuhangaika kulia na kushoto, madhaifu na wanyonge!

5 Na milima itakuwa kama sufi iliyo tiwa rangi na kuchambuliwa kwa kutapanyika vipande mbali mbali na kupeperuka katika anga huku na huku.

6 Ama yule ambaye mizani yake itakuwa nzito, mema yake yakapindukia kuliko maovu yake, basi huyo atakuwa na maisha yatayo mridhisha mwenyewe, na nafsi yake itue.

7 Tazama tanbihi 6.

8 Na ama ambaye mizani yake itakuwa nyepesi, na maovu yake yakazidi kuliko mema yake, basi makaazi yake yatakuwa Jahannamu.

9 Tazama tanbihi ya 8.

10 Na nini cha kukujulisha ni nini Hawiya?

11 Moto ulio mkali, hapana moto unao fikilia ukali wake, hata ukichochea vipi na kutiwa kuni gani.

Sura 102 - At-Takaathur

Utangulizi

Sura hii inawaibisha wale ambao kushindania wingi kumewashughulisha na kutimiza yaliyo ya waajibu. Na inawaonya kwamba hakika watakuja jua mwisho wa taksiri yao hiyo, na inawakhofisha watu kuwa watakuja uona Moto na watakuja ulizwa neema walizo kuwa nazo.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Kumekushughulisheni kutafuta wingi,¹
2. Mpaka mje makaburini!²
3. Sivyo hivyo! Mtakuja jua!³
4. Tena sivyo hivyo! Mtakuja jua!⁴
5. Sivyo hivyo! Lau mngeli jua kwa ujuzi wa yakini,⁵
6. Basi bila ya shaka mtaiona Jahannamu!⁶
7. Tena, bila ya shaka, mtaiona kwa jicho la yakini.⁷
8. Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema.⁸

1 Yamekushughulisheni mkaacha kutimiza yaliyo waajibu na ya ut'iifu kule kujitapa kwenu kwa wana na wafwasi, na kujifakhiri kwa mali, na hisabu, na nasaba, mpaka yakusibuni mauti.

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Hakika mtakuja jua matokeo ya upumbavu wenu na mapuuzwa yenu.

4 Na hakika bila ya shaka mtakuja jua natija ya hayo!

5 Ama kwa hakika lau mngeli jua kwa yakini uovu wa mwisho wenu bila ya shaka mngeli ogopa huko kushindania kurindika mali, na mngeli jitengenezea Akhera yenu.

6 Nakuapieni na nakutilieni mkazo, enyi watu, kwamba hakika nyinyi mtakuja ushuhudia Moto unao waka.

7 Kisha ninaapa na natilia mkazo kwamba mtaiona wazi na kwa yakini.

8 Tena naapa na natilia mkazo kwamba hakika nyinyi mtahisabiwa kwa neema mlizo deka nazo na mkazistarehea.

Sura 103 - Al-'As'r

Utangulizi

Katika Sura hii anaapa *Subhanahu* kwa Zama, kwa zilivyo kusanya chungu ya ajabu, na mazingatio yenye kujuulisha uweza wa Mwenyezi Mungu na hikima yake, ya kwamba mtu haachi kuwa na upungufu katika vitendo vyake na hali zake ila Waumini wanao tenda mema, na wakausiana kushika Haki. Na hiyo ndiyo kheri yote. Na wakausiana kusubiri na kuvumilia juu ya walio amrisha na walio katazwa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Naapa kwa Zama!¹
2. Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika khasara,²
3. Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri.³

1 Naapa kwa Zama kwa sababu ya maajabu mengi na mazingatio yaliomo ndani yake.

2 Hakika kila binaadamu bila ya shaka yumo katika namna fulani au fulani ya kukhasiri, kwa mujibu wa anavyo ghilibiwa na pumbao na matamano.

3 Isipo kuwa wale walio muamini Mwenyezi Mungu na wakatenda mema, na wakadumu juu ya ut'iifu, na wakasemezana na kuusiana kwa kushikamana na Haki, kwa itikadi, na maneno, na vitendo. Na wakausiana wasubiri na wavumilie mashaka yanayo wapata wenye kushikamana na Dini. Basi hao ndio wenye kusalimika na hiyo khasara, wenye kufanikiwa duniani na Akhera.

Sura 104 - Al-Humazah

Utangulizi

Katika Sura hii kipo kitisho kikubwa kwa mwenye kuzoea kuwakebehi watu kwa ishara au kwa maneno, mwenye kukusanya mali mengi, akayahisabu kwa ajili ya fakhari, na kudhani kuwa mali yake yatambakisha milele duniani.

Na humo vile vile lipo onyo kubwa kwa hao kuwa watatiwa kwenye Moto mkali unao vuruga miili yao na nyoyo zao, na wanafungiwa milango, na juu ya hivyo watafungwa pingu humo basi hawataweza kutaharaki wala kutoka.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Ole wake kila safihi, msengenyaji!¹
2. Aliye kusanya mali na kuyahisabu.²
3. Anadhani ya kuwa mali yake yatambakisha milele!³
4. Hasha! Atavurumishwa katika H'ut'ama.⁴
5. Na nani atakujavya ni nini H'ut'ama?⁵
6. Moto wa Mwenyezi Mungu ulio washwa.⁶
7. Ambao unapanda nyoyoni.⁷
8. Hakika huo utafungiwa nao⁸
9. Kwenye nguzo zililo nyooshwa.⁹

1 Atapata adhabu kali na maangamio huyo ambaye mtindo wake ni kuwafedhehi watu kwa kauli au kwa ishara, au kuwasengenya kuwavunjia hishima zao.

2 Ambaye amekusanya chungu ya mali na akawa kazi yake kuyahisabu tu, kwa kuona ladha huko kuhisabu.

3 Anadhani huyo kuwa mali yake yatamweka milele duniani, na yatamkinga na hayo anayo yachukia?

4 Na aache dhana hiyo! Wallahi! Hapana shaka yoyote kwa vitendo vyake viovu hivyo atakuja tumbukizwa katika Moto unao vuruga kila kinacho tupwa humo!

5 Na kitu gani kitacho kujavya nini ukweli wa Moto huu wa H'ut'ama?

6 Moto wa Mwenyezi Mungu ulio washwa kwa amri yake, na daima unawaka.

7 Ambao unafikilia nyoyoni na kuzizunguka nyoyo.

8 Huo utakuwa umefungwa milango yake, na wao watakuwa wamefungwa humo ndani kwenye maguzo yaliyo nyooka. Hawawezi kutaharaki, wala kutoka.

9 Tazama tanbihi ya 8.

Sura 105 - Al-Fiil

Utangulizi

Mwenyezi Mungu anampa khabari Mtume wake s.a.w. kisa cha Watu wa Tembo (Ndovu) walio kusudia kuivunja Nyumba ya Mwenyezi Mungu ya Al-Kaa'ba, na anakionyesha kisa hichi kuwa ni dalili ya uweza wake Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kujilipizia kwake juu ya hao wanao vunja vitu vyake vitakatifu. Mwenyezi Mungu hakika aliwasalitishia majeshi yalio wang'oa mizizi yao, na wasibakie kitu ila kama nazi iliyo liwa na mwezi.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Kwani hukuona jinsi Mola wako Mlezi alivyo watenda wale wenye tembo?¹
2. Kwani hakujaalia vitimbi vyao kuharibika?²
3. Na akawapelekea ndege makundi kwa makundi,³
4. Wakiwatupia mawe ya udongo wa Motoni,⁴
5. Akawafanya kama majani yaliyo liwa!⁵

1 Hakika, ewe Muhammad, unajua kwa ujuzi usio ingiliwa na shaka yoyote, alivyo fanya Mola wako Mlezi kuwafanyia wale watu wenye tembo (ndovu), wakataka kuishambulia Nyumba takatifu ya Al-Kaaba.

2 Unajua ya kwamba hakika Mwenyezi Mungu amejaalia juhudi yao kutaka kuibomoa Al-Kaaba ivize na ipotelee mbali. Juhudi yao ikapeperuka, na wao wasipate makusudio yao.

3 Na Mwenyezi Mungu aliwasalitisha na majeshi ya ndege yaliyo watokea makundi kwa makundi yakifuatana, na yakawazunguka kila upande.

4 Wakiwatupia mawe kutoka Jahannam.

5 Akawafanya kama majani ya mimea yaliyo sibiwa yakatilifu.

Sura 106 - Quraish

Utangulizi

Mwenyezi Mungu katika Sura hii anataja neema alizo wafanyia Maqureshi kwa Nyumba yake takatifu ambayo ameilinda na maadui wake, naye akawapa maskani karibu yake wakapata utukufu na amani, na wakawa wanasafiri siku za baridi kwenda Yaman, na siku za joto wakenda Shamu, kwa ajili ya biashara bila ya mtu yeyote kuwaletea maovu, na hali watu jirani zao siku zote wakinyakuliwa. Na neema hizo zinawajibikia kumuabudu huyo aliye kuwa anawalisha wasipate njaa, na akawalinda na khofu.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Kwa walivyo zoea Maqureshi,¹
2. Kuzoea kwao safari za siku za baridi na siku za joto.²
3. Basi nawamuabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii,³
4. Ambaye anawalisha wasipate njaa, na anawalinda na khofu.⁴

1 Hebu staa jabuni kwa yanayo walazimu Makureshi! Kuwalazimu safari za musimu wa baridi kwenda Yaman, na safari za musimu wa joto kwenda Shamu, kufanya biashara na kutafuta riziki kwa utulivu na amani. (Hizo safari za biashara za Yaman ndizo zilizo waleta Waarabu Afrika Mashariki kwa maelfu ya miaka, na zikauleta Uislamu pande za Afrika kabla ya kuenea Arabuni. Kwani nchi za Afrika Mashariki zilikalikiwa na Waarabu kwa maelfu ya miaka. Soma *Periplus of the Erythrean Sea, na East Africa and Its Invaders* ya Prof. Coupland, na vitabu vya Sir John Gray na Dr. L.W. Hollingsworth.)

2 Tazama tanbihi ya 1.

3 Basi wamtakasie ibada Mola Mlezi wa Nyumba hii aliye wawezesha kuzifanya hizi safari mbili.

4 Ambaye anawalisha wasipate njaa, na hali wao wamo katika bonde lisio na makulima, na akawalinda na khofu na watu wengine pembezoni mwao wananyakuliwa.

Sura 107 - Al-Maau'n

Utangulizi

Sura hii inahadithia khabari za mwenye kukadhibisha malipo ya Akhera. Ikataja katika sifa zake kuwa yeye anamdhaliisha yatima, na anamkemea kwa ukali, si kwa kumtengeza. Na kwamba yeye hamhimizi mtu yeyote, la kwa kauli wala kwa kitendo, kuwalisha masikini; kwa sababu huyo ni mchoyo kwa mali yake, bakhili kwa alichu nacho mkononi. Kisha Sura imewataja watu wa kikundi kingine wanao shabihiana na hawa wanao kadhibisha malipo. Hawa ni wale wanao ghaflika na Sala zao, ambao hawasali kama itakikanavyo, na ambao husimama kwa hayo kwa dhaahiri tu si kwa hakika. Ni wenye kuonyesha tu a'mali zao, wenye kuzuia msaada wao wasiwape wanao hitajia. Na Sura inawaahidi hao kuwa watapata misiba na maangamio, ili waache uasi wao.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Je! Umemwona anaye kadhibisha Malipo?¹
2. Huyo ndiye anaye msukuma yatima,²
3. Wala hahimizi kumlisha masikini.³
4. Basi, ole wao wanao sali,⁴
5. Ambao wanapuza Sala zao;⁵
6. Ambao wanajionyesha,⁶
7. Nao huku wanazuia msaada.⁷

1 Unamjua anaye kanusha malipo na hisabu ya Akhera?

2 Ukitaka kumjua basi ni huyo ambaye anaye msukuma yatima kwa nguvu, na anamtumilia mabavu, na anamdhulumu, na wala hahimizi kulishwa masikini.

3 Tazama tanbihi ya 2.

4 Maangamio yatawashukia wanao sali na wakasifika kwa sifa hizi, na wakaghaflika na Sala zao wasinafike nazo.

5 Tazama tanbihi ya 4.

6 Ambao huonyesha kwa watu vitendo vyao, ili wapate cheo katika nyoyo za hao watu, na wasifiwe.

7 Na huku wanazuia hisani zao na msaada wao kwa watu.

Sura 108 - Al-Kawthar

Utangulizi

Mwenyezi Mungu katika Sura hii anamtajia Mtume wake s.a.w. neema alizo mfanyia kwa kumpa kheri nyingi na neema kubwa kubwa katika dunia na Akhera, na akamtaka adumishe Sala iliyo safi kwa kumridhi Mwenyezi Mungu, na atoe mhanga bora ya mali yake kwa dhahiya ya shukrani kwa ukarimu alio pewa. Kisha Sura imekhitimisha kwa kumbashiria Nabii s.a.w. kuwa atakatiliwa mbali huyo anaye mchukia na kumbughudhi Mtume.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Hakika tumekupa kheri nyingi.¹
2. Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi.²
3. Hakika anaye kuchukia ndiye aliye mpungufu.³

1 Sisi hakika tumekupa kheri nyingi za daima katika dunia na Akhera.

2 Ilivyo kuwa umepewa hayo, basi dumisha Sala kwa Mola wako Mlezi kwa usafi kabisa, na uchinje dhabihu wako kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa aliyo kupa ya ukarimu, na akakukhusisha wewe khasa kwa kukupa kheri.

3 Hakika huyo anaye kuchukia ndiye aliye katika na kila kheri.

Sura 109 - Al-Kaafirun

Utangulizi

Katika Sura hii Mwenyezi Mungu anamuamrisha Mtume wake s.a.w. awakatishe tamaa makafiri katika juhudi zao za kutaka kusikilizana na Mtume katika wito wake wa Haki, kwa kuwa yeye ni mwenye kubakia vile vile juu ya ibada ya Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu ila Yeye, na wao wabakie kuiabudu miungu yao ambayo haifidi chochote katika Haki, wao wawe na dini yao walio ifuata baba zao, na yeye na Dini yake aliyo mridhia Mwenyezi Mungu aifuata.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Sema: Enyi makafiri!¹
2. Siabudu mnacho kiabudu;²
3. Wala nyinyi hamuabudu ninaye muabudu.³
4. Wala sitaabudu mnacho abudu.⁴
5. Wala nyinyi hamuabudu ninaye muabudu.⁵
6. Nyinyi mna dini yenu, nami nina Dini yangu.⁶

1 Ewe Muhammad! Sema: Enyi makafiri, mlio shikilia juu ya ukafiri wenu.

2 Mimi simuabudu mnaye muabudu nyinyi badala ya Mwenyezi Mungu.

3 Wala nyinyi si wenye kumuabudu huyo ambaye mimi namuabudu, naye ni Mwenyezi Mungu wa pekee.

4 Wala mimi si mwenye kuabudu mfano wa ibada yenu, kwani nyinyi ni washirikina.

5 Wala nyinyi si wenye kuabudu mfano wa ibada yangu, kwani hii ni Tawhidi, ibada ya Mungu Mmoja.

6 Nyinyi mna dini yenu mnayo itakidi, na mimi nina Dini yangu aliyo niteulia Mwenyezi Mungu niishike.

Sura 110 - An-Nas'r

Utangulizi

Sura hii imemtaka Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w. ukija msaada wa Mwenyezi Mungu na ushindi, na akaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi kwa kutua mambo yake na kutukuka neno lake na kumkamilishia Mwenyezi Mungu, basi amtakase Mola wake Mlezi kwa kumsifu, na amtakase na kila lisio mwelekea, na amwombe msamaha kwa nafsi yake na kwa Waumini, kwa sababu hakika Yeye ni Mwingi wa kukubali toba za waja wake, na anasamehe makosa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi,¹
2. Na ukaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi,²
3. Zitakase sifa za Mola wako Mlezi, na umwombe msamaha; hakika Yeye ndiye anaye pokea toba.³

1 Ikithibiti nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi kwako na kwa Waumini,

2 Na ukawaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu makundi kwa makundi,

3 Basi mshukuru Mola wako Mlezi, na Sabbih', Mtakase kwa sifa zake, na mtake akusamehe wewe na umma wako, kwani hakika Yeye ni Mwingi wa kupokea toba za waja wake. (*Tazama* Maelezo 110:3)

Sura 111 - Al-Masad

Utangulizi

Sura imeanza kwa kutoa khabari kuhiliki kwa Abu Lahab, adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kuwa hapana kitu cha kumfaa, mali wala cheo au vyenginevyo, na inamuhidi kuwa Akhera ataingia Motoni na ataungua humo, pamoja na mkewe ataye kuwa naye. Na yeye amekhusishwa kwa adhabu ya kufungwa kamba katika shingo yake ya kumvutia mpaka kwenye Moto katika kuzidi kumuadhibu kwa sababu ya maudhi yake aliyo kuwa akimfanyia Mtume na maovu aliyo kuwa akiyafanya kupinga Wito.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Imeangamia mikono ya Abu Lahab, na yeye pia ameangamia.¹
2. Hayatamfaa mali yake, wala alivyo vichuma.²
3. Atauingia Moto wenye mwako.³
4. Na mkewe, mchukuzi wa kuni,⁴
5. Shingoni mwake iko kamba iliyo sokotwa.⁵

1 Imeteketa mikono ya Abu Lahab iliyo kuwa ikiwadhi Waislamu, na yeye mwenyewe amehiliki pia.
2 Hayatolindwa na adhabu ya Mwenyezi Mungu mali yake aliyo kuwa nayo, wala cheo chake alichokichuma.
3 Ataingia katika Moto unao waka, aungue.
4 Na ataingia pia kwenye Moto mkewe huyo aliye kuwa akibeba masengenyo baina ya watu, kama alivyoingia yeye (mumewe)
5 Juu ya shingo yake itakuwa kamba ya mtende ya kumtesa.

Sura 112 - Al-Ikhlās'

Utangulizi

Nabii s.a.w. aliulizwa khabari za Mola wake Mlezi, akaamrisha katika Sura hii ajibu kwamba Yeye ni Mwenye kukusanya sifa zote za ukamilifu, ni Mmoja, wa Pekee, Mwenye kukusudiwa daima katika haja, Mwenye kujitoshia hamhitajii yeyote mwengine, ametakasika na kuwa na mfano, hakuzaa wala hakuzaliwa, wala hana mwenzie katika viumbe vyake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee.¹
2. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa.²
3. Hakuzaa wala hakuzaliwa.³
4. Wala hana anaye fanana naye hata mmoja.⁴

1 Ewe Muhammad! Hao wanao sema kwa kejeli, "Tusifia Mola wako Mlezi.": waambie: Yeye ni Mwenyezi Mungu wa pekee hapana mwengine, wala hana mshirika.

2 Mwenyezi Mungu Mwenye kukusudiwa peke yake katika haja zote, na yote yanayo takikana.

3 Hana mtoto wala hakuzaliwa na baba wala mama, wala hana yeyote aliye mshabihi, au mfano wake.

4 Tazama tanbihi ya 3.

Sura 113 - Al-Falaq

Utangulizi

Sura hii inamtaka Nabii s.a.w. amwendee Mola wake Mlezi atake ulinzi kwake kujilinda na shari ya kila mwenye shari, ya viumbe vyake, na shari za usiku linapo ingia giza, yanayo yasibu nafsi katika hali ya upweke, na madhara ambayo mtu hawezi kujikinga nayo, na shari za mafisadi wanao pita kuharibu makhusiano na mawasiliano yalio baina ya watu, na shari za hasidi anaye tamani kuondoa neema alizo wapa Mwenyezi Mungu waja wake.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa mapambazuko,¹
2. Na shari ya alivyo viumba,²
3. Na shari ya giza la usiku liingiapo,³
4. Na shari ya wanao pulizia mafundoni,⁴
5. Na shari ya hasidi anapo husudu.⁵

1 Sema najikinga na Mola Mlezi wa asubuhi inapo pambazuka kutokana na usiku.

2 Na shari ya kila chenye shari katika viumbe, ambavyo hapana wa kuzuia shari yao ila Mwenye kumiliki amri yao.

3 Na shari ya usiku unapo kuwa totoro.

4 Na shari ya anaye pita baina ya watu kwa sababu ya kuwafisidi.

5 Na shari ya hasidi anaye tamani iondoke neema kwa wengine.

Sura 114 - An-Naas

Utangulizi

Katika Sura hii Mwenyezi Mungu anamuamrisha Nabii wake s.a.w. amwendee Yeye amwombe ulinzi kumkinga na shari kubwa zinazo washinda watu wengi kuzitambua kwa sababu zinatokana na matamania yao, na pumbao lao, basi wakatumbukia katika yale yale wanayo katazwa.

Hiyo ndiyo shari ya wasiwasi wa Shetani, anaye jificha machoni, au hujidhihirisha kwa kificho; wasiwasi wake ni kwa hila na khadaa.

*** **

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

1. Sema: Ninajikinga kwa Mola Mlezi wa wanaadamu,¹
2. Mfalme wa wanaadamu,²
3. Mungu wa wanaadamu,³
4. Na shari ya wasiwasi wa Shetani, Khannas,⁴
5. Anaye tia wasiwasi katika vifua vya watu,⁵
6. Kutokana na majini na wanaadamu.⁶

1 Sema: Najikinga na Mola Mlezi wa wanaadamu, Mwenye kuendesha mambo yao.

2 Mfalme wa wanaadamu, kwa ufalme ulio timia, kuwamiliki wote wafalme wao na maraia.

3 Mungu wa wanaadamu, Mwenye uweza kwa kuwasarifu kwa ukamilifu atakavyo.

4 Na shari ya mwenye kutia wasiwasi watu, ambaye hurudi nyuma ukiomba msaada kwa Mwenyezi Mungu dhidi yake.

5 Ambaye hutia kwa kificho katika vifua vya watu ya kuwaachisha wasende kwenye njia ya uwongofu.

6 Kutokana na majini na wanaadamu.

*Mwisho wa Qur'ani Tukufu. Kurasa zinazokuja zina
'Maelezo Zaidi ya Aya' na 'Orodha ya Maneno'.*

Maelezo Zaidi ya Aya

Haya ni maelezo zaidi juu ya baadhi ya aya. Kwa mfano, 1:7 ni maelezo zaidi kuhusu sura ya kwanza, aya ya 7, na 2:22 ni maelezo zaidi kuhusu sura ya pili, aya ya 22.

1:7 - Hapana katika Vitabu vyote vitakatifu, vya dini zote, dua inayo lingana na hii kwa uzuri wake, na utimilivu wake. Baada ya kumsifu Mwenyezi Mungu kwa Rehema yake isio na ukomo wala kipimo, na kumshukuru Mola Mwenye kuviumba na kuviangalia na kuvilea kwa huruma viumbe vyote, na kuhakikisha kuwa tunajua kuwa hapana Mungu ila Yeye tu wa kuabudiwa na kuombwa msaada, na kuwa hapana wa kumingilia katika Ufalme wake na Uwezo wake wa kulipa hisabu kwa kila alitendalo mtu, hapo tena ndio tunaomba. Na tunaomba nini? Si mkate wa kula, wala riziki yoyote, wala jambo lolote la manufaa ya kimwili duniani, bali tunaomba Uwongofu kwenye Njia Iliyo Nyooka, Njia ya kumwendea Yeye Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema. Tunaomba tusiendee njia waliyo ifuata wale walio kasirikiwa na Mwenyezi Mungu, kwa kuwa walifunzwa wakajua, lakini kwa chuki na jeuri wakakataa kuongoka, wala sio njia ya wale ambao labda kwa ujinga wamepotea. Hiyo kwa mukhtasari ndiyo Dua ambayo Waislamu, wanafunzwa waiombe, na wanaiomba mara kadhaa wa kadhaa katika Sala zao, na katika kila fursa inapo tokea.)

2:22 - Katika Aya hii ipo sehemu ya kuonesha muujiza wa Qur’ani Tukufu: nayo ni kauli yake Mtukufu “mbingu kama paa”. Haya asingeyajua Nabii asiyejua kusoma ila kwa ufunuo wa Mwenyezi Mungu, nayo ni kuwa mbingu kwa kisayansi ni kila kilicho izunguka dunia pande zote, na kwa ukomo wowote, na kwa yoyote katika anga, mpaka huko juu kabisa kwenye sayari nyenginezo, zilizoenea zisio na mwisho. Zote hizo zinazunguka kwa mpango wa ajabu, na sisi tunapata uvukuto na mn’gao wake, nazo zinakwenda kwa nguvu ya mvutano kama smaku. Katika sehemu ya mwanzo ya mbingu iliyo tuzunguka lipo anga linalo tuinga kama paa na mianga inayo dhuru kutokana na hizo sayari. Na tabaka hizo huachilia mianga yenye faida tu, ndipo penye mawingu yaletayo mvua.

2:40 - Aya hii inaonyesha kuwa ahadi, au agano, ni waajibu wa pande zote mbili zilizo ahidiana kutimiza lilio lazimika. Akiacha mmojapo basi haimlazimu wa pili kutimiza agano lake.

2:51 - “Masiku” ni wingi wa Usiku. Wingi wa siku ni siku, kama ilivyo sahani, sabuni, silaha, sinia, sungura, saa. Ni makosa kwa Kiswahili kusema “masiku” kuwa ni wingi wa siku; “Masiku” ni wingi wa “Usiku”. Kutumia “Masaa” kuwa ni wingi wa “Saa” ni makosa.

2:57 - Katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Na tukakuteremshieni Manna na Salwa” imetajwa kwa uhakika wa kisayansi, kwani hivi mwishoni imevumbuliwa kuwa madda za “Protein” zenye asli ya vinyama kama vile nyama na ndege ni bora kumfaa mtu kwa chakula kuliko “Protein” zinazotoka katika mimea na mboga. Na katika Manna mna sukari ya kumpa mtu nguvu na uchangamfu wa kufanyia kazi na

kutaharaki huku na huku.

2:73 - Mwandishi mmoja wa zama zetu, marehemu Sh. Abdul Wahhab Annajjar ametaja kwamba kauli ya Mwenyezi Mungu: “Mpigeni kwa kipande chake” maana yake kipande cha aliye uwawa. Na makusudio ya kufufuka kwake ni kumtolea kisasi, kwa kuwa kupigwa kwa kiungo cha mwenye kuuliwa humpelekea muuwaji kuungama, na mara nyingi kumwona tu aliye uwawa humpelekea mwenye kuuwa kuungama. Na inakuwa kisa hichi ni mbali na lile jambo la kuchinja, na kuamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kuchinja; na kwamba kuamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu wamchinje ng’ombe ni kwa ajili ya kumla. Na katika haya pana mafunzo ya nafsi kwao, kwani hawa walikuwa pamoja na Wamisri ambao wakimwona ng’ombe ni mtakatifu, na yalikuwa kwao mabaki ya haya ya kumtukuza ng’ombe kwa dalili ya kuwa waliabudu sanamu la ndama baada ya hayo. Ikawa hapana budi kung’oa mabaki yake katika nafsi zao kwa kuwalazimisha kumchinja ng’ombe. Ndio ikawa ile amri ya kuchinja, na yakatokea majadiliano na kukawa kule kusitasita kwao, na mwisho wakamchinja, na walikaribia wasichinje.

2:85 - Kabla ya Uislamu zilikuwapo katika mji wa Madina kabila mbili za Kiarabu ambazo zilikuwa na uadui baina yao, nazo ni Aus na Khazraj. Na pia zilikuwako kabila za Kiyahudi nazo ni Banu Quraidha na Banu Nnadhira. Banu Quraidha walifungamana na Aus, na Banu Nnadhira walifungamana na Khazraj. Ilikuwa kabila mbili za Kiarabu zikipigana, zile kabila za Kiyahudi nazo huingia vitani, kila kabila upande wa rafiki zake, na zikiuwana na wenzao wa dini moja nao, na wakifukuzana makwao. Lakini kila moja katika kabila mbili hizo za Kiyahudi zikishughulika baadaye kuwakomboa mateka walio tekwa na rafiki zao wa Kiarabu. Wakiulizwa kwa nini mnawakomboa na hao walikuwa wakipigana nanyi upande wa maadui zenu? Wao wakisema: Mwenyezi Mungu ametuamrisha katika Taurati tuwakomboa mateka wa Kiyahudi. Na wanajifanya hawajui kama Mwenyezi Mungu amewaamrisha vile vile wasiuwane wala wasitoane majumbani mwao. Kwa hivyo ndio wanaamini sehemu ya Kitabu na wanaikataa nyengine.

2:89 - Mwenyezi Mungu alimwambia Musa: “Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe...mtu asiye sikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake.” (Kumbukumbu la Torati 18.18-22.) Maana ya haya ni: Taurati inasema kwamba Nabii Musa aliambiwa na Mungu kwamba atawaletea Nabii kutokana na ndugu za Wana wa Israili, yaani Waarabu. Na asiye mfuata Nabii huyo Mwenyezi Mungu atamuadhibu.

2:104 - Katika lugha ya Kiyahudi ya Kiebrania lipo neno “Rai’nu” ambalo limejengwa na neno “Ra” kwa maana ya “Shari” na neno “nu” linaonesha jamii, wingi. Na maana ya neno lote ni kuwa “Wewe ni shari yetu”, wakikusudia kumwambia Mtume hayo.

2:129 - Mwenyezi Mungu hakupeleka Mtume kutokana na vizazi vya Ismail ila Muhammad s.a.w. Kwake yeye ndiyo dua hii imepokelewa na Mwenyezi Mungu kwa kutumwa kwa vizazi vya Ismaili na wanaadamu wote.

2:145 - Wanasema wafasiri kuwa Mayahudi wanaelekea kwenye Mwamba katika Beitul Muqaddas na Wakristo wanaelekea Mashariki.

2:172 - Qurani imeutangulia utibabu wa kisasa kwa kukataza kula mzoga, kwani kifacho kwa ukongwe au ugonjwa husabibishwa na sumu inayo mdhuru mlaji. Kadhaalika cha kunyongwa au maradhi huinajisi damu, na ndani yake huwamo vingi vya kudhuru kama jasho na mkojo. Na nguruwe husabibisha maradhi ya khatari kama TRICHINOSIS ambayo khatimaye huharibu moyo na mapafu na husabibisha mauti.

2:173 - Hali ya dharura inaruhusisha kinacho harimishwa, kwa sababu mauti ya yakini yanashinda madhara yanayo weza kustahamilika, na kwamba mwenye kulazimika kwa dharura haimfalii kupindukia mpaka wa dharura, wala asikiuke kile alichu lazimika kukila.

2:178 - Waarabu zama za jahiliya walikuwa hawafanyi usawa baina ya watukufu na wanyonge. Akiuliwa mwongozi hawatosheki na kumuwa muuwaji bali huyo huachwa akenda kulipizwa kisasi kwa mwongozi wa kabila ya muuwaji. Kwao roho si sawa, na damu si sawa. Uislamu haukukubali haya, lakini ukapasisha Kisasi, roho kwa roho, mwenye kuuwa huuwawa. Muuwaji yeyote awaye atauliwa akiwa muungwana, mtumwa au mwanamke. Haya ni kwa ajili ya usawa katika damu; hapana mwenye damu tukufu na damu isiyo tukufu. Na inafahamika kwa ishara kuwa nafsi kwa nafsi. Na hii ni sharia ya milele, ilikuwako katika Taurat, na Injil na Qur'ani. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: "Na tuliwaandikia kuwa nafsi kwa nafsi..." (taz. Almaida). Na Mtume s.a.w. amesema: "Damu za Waislamu ni sawa." Na amesema: "Nafsi kwa nafsi". Zingatia: Uislamu kwa sharia ya kisasi ina nadhari nyengine, sio kama kanuni za kutungwa. Imewapa wenye kuuliwa mtu wao haki ya kutaka muuwaji auwawe, kuondoa fitna na umwagaji wa damu mkubwa. Imewapa haki ya kusamehe au kulipwa kisasi, wala haizuilii serikali kumfedhehi aliye uwa ikiona hivyo ni maslahu. Uislamu hauzingatii sababu ya kuuwa, kwani mwenye kuuwa amedhulumu hata ikiwa sababu gani. Na huenda ukitafta sababu akaonewa huruma mkosa, na kumpuuzwa mkoswa. Na hayo hupelekea mchafuko wa watu kuchukua kisasi mkononi mwao, na kuzalikana makosa juu ya makosa ya kuuwa, kwa kutoridhika wale walio uliwa mtu wao. Nadharia hii ya Kiislamu sasa inaduruswa katika vyuo vikuu vya Ulaya.

2:185 - Imethibiti kwa matibabu ya kisasa kuwa Saumu kwa namna ya Qur'ani ina faida nyingi, katika hizo ni kuwa inasaidia katika kutibu maradhi ya sukari, inatengeneza matumbo, inapunguza maumivu ya viungo, na maradhi ya moyo, inapumzisha nyama za mwili, na inasafisha uchafu mwingi wenye madhara, na pia inakuwa ni kinga kwa maradhi mengi mengineyo. Je, vipi kwa mtu asiye jua kusoma na kuandika ayajue yote haya?

2:189 - Uislamu unahisabu mwezi unapo andama na kugeuka kwa watu kupimia nyakati za ibada, na pia kwa mambo yao ya kidunia, kwa sababu hayo ni mambo ya kuonekana, na kwa hivyo taarikihi inajulikana kwa sura ya mwezi. Mwezi kwa hakika ni kama kioo kinacho onyesha mwangaza wa jua huku duniani. Mwezi ukiwa

kati baina ya jua na dunia hauonekani, na baadae mwezi mchanga unaandama na wakaazi wa dunia wanajua kuwa mwezi mpya umeanza. Ukifika mwezi katika upande unao kabiliana baina ya jua na dunia ndio unapo kuwa wakati wa mbaamwezi, mwezi mpevu. Khalafu unaendelea kupungua kama ulivyo kuwa kwanza ukizidi kukua. Kwa hivyo taarikhi inaanza tangu pale ulipo kuwa mwezi mchanga. Pale unapo onekana mwezi mchanga kama uzi ndio mwezi umeandama, huonekana upande wa magharibi, hata kwa dakika chache baada ya kuchwa jua nao hupotea. Hivyo hivyo siku baada ya siku huhisabiwa mpaka zipite siku 29 au 30.

2:195 - Aya 190 mpaka 195 zinaeleza sharia ya vita katika Uislamu. Nazo zinaeleza kwa matamshi yalio wazi haya yafuatayo:

*1. Ruhusa ya kupigana imetolewa kwa ajili ya kujilinda na uvamizi wa vita wa vitendo khasa, au zikidhihiri dalili kuwa maadui wanataka vita. Vita havikulazimishwa kwa ajili ya vita wala kwa sababu ya kutaka kuwasilimisha watu kwa kuwauwa na kuwapiga vita.

*2. Kunakatazwa kuvamia au kuanza uadui kwa njia yoyote ile. Basi hapana ruhusa kufanyiwa uadui asiye pigana, wala hapana ruhusa kuvuka mipaka ya uadui wakati wa vita: basi hauliwi asiye chukua silaha, wala hakhusiani na vita bali ni mwenye kukumbwa tu na vita. Wala hauliwi mwenye kusalimu amri na akatupa silaha. Wala hapana ruhusa kuwavunjia watu nyumba zao, huko ni kupita mpaka.

*3. Mzingatie fadhila iliyo onyeshwa kwa kuamrisha kuchamngu. Basi msivunje heshima ya wanawake kuwanajisi, hata washirikina wakifanya hayo. Wala msiwakatekate walio uwawa hata ikiwa makafiri wakiwafanyia hayo Waumini. Washirikina walimfanyia hayo Bwana wa Mashahidi, Hamza, wala Mtume s.a.w. hakutoa ruhusa kumfanyia hayo maiti yeyote, bali alikataza akasema: "Tahadharini msiwakatekate maiti".

*4. Vita vinakwisha wakiacha washirikina kuwafitini Waumini katika Dini yao, na Dini inakuwa inataka akili na nyoyo zimwelekee Mwenyezi Mungu kwa uhuru.

*5. Hapana vita katika mwezi mtukufu, nayo ni miezi ya Hija na Umra. Ikiwa washirikina watapigana katika miezi hiyo, basi Waumini nao yawapasa wapigane.

*6. Kuacha kutoka kwenda pigana na maadui wanauwa pasina nasi kupigana nao ni kuipoteza kheri na wema. Kwa haya inadhihiri kuwa vita vya Islamu vina fadhila katika sababu zinazo pelekea kuanza kwake, na vina uadilifu katika kuviendesha. Viwapi hivi na vita vya mataifa mengine ya zamani na ya sasa! Vita vyao hao ni vya uchafu, na vita vya Islamu ni vya Haki na vyenye fadhila.

2:203 - Hayo mawe ni changarawe hutupwa mwahala maalumu katika Mina katika siku ya kuchinja (Idd) na siku tatu zifwatazo.

2:208 - Maneno haya ya Qur'ani ni wito kwa Waumini wote iwe baina yao salama na amani, na yanafahamisha kuwa vita na khasama ni katika mwendo wa kumfuata Shetani. Waumini wote wanaitwa wawe katika hali ya salama na wengineo, na wao baina yao kwa wao, wasipigane na wengine wala wasipigane wenyewe kwa wenyewe. Na maneno haya ya Qur'ani yanaonyesha kuwa mahusiano baina ya dola ya Kiislamu na nyenginezo ni salama, na huo ni msingi wa mwanzo wa dini zote za mbinguni.

Wakati ilipo kuwa kanuni ya porini ndiyo inayo hukumu baina ya madola na kuwekea mipaka ya mahusiano yao, mwenye nguvu kumla mnyonge, Uislamu ulikuja na huu msingi wa kuamrisha kuwa mahusiano yawe ya Usalama. Pindi vikitokea vita basi viwe kwa ajili ya ulinzi na kuupinga uvamizi. Yaani ni kumlazimisha yule mwenye kufanya uadui awe mwenye usalama. Vita vilivyo ruhusywa na Uislamu ni kuthibitisha nguzo za amani, na kuhakikisha uadilifu. Vita hivi ni vita vya salama, kwa ajili ya uadilifu na amani.

2:219 - Kifungu hichi cha Qur’ani kinatuwekea wazi makusudio ya sharia ya Kiislamu. Kinatueleza kuwa sharia inataka manufaa ya waja. Chenye kuzidi nafuu yake kuliko madhara kinafaa. Chenye nafuu chache kuliko madhara kinakatazwa. Pia kifungu kinatonyesha kuwa vitu ulimwenguni vimechanganya mema na mabaya. Hapana ovu lisio kuwa na wema, wala wema usio na uovu. Ulevi, mama wa maovu, unao haribu akili na kumfanya mtu kuwa mnyama, nao una faida pamoja na uovu wake usio na mpaka. Na kamari inayo shughulisha nafsi na akili, ikaleta mpapatiko usio sita, nayo ina nafuu yake pamoja na kuwa na madhambi yanayo fisidi maisha na nyumba za watu, na kila makhusiano bora ya binaadamu.

2:222 - Ilimu za kisasa zimethibitisha kuwa wakati wa hedhi yanaweza kuwa madhara kwa kuwa zalio huweza kupata maradhi pindi likiingiliwa na vidudu vya maradhi, ambavyo ni vyepesi kuingia wakati wa kuingiliana na mwanamume. Maradhi hayo huenda yakasababisha mwanamke asiweze kuzaa. Mwanamume naye huambukia maradhi hayo kutokana na mwanamke kwa kupitia njia za mkojo, na maradhi yakapanda juu mpaka mafigo yakaharibika, na kuathirika vyombo vya uzazi, na mwanamume naye akawa hawezi kutia mimba. Maradhi haya huleta machungu makubwa. Watu walikuwa hawajui, lakini Mwenyezi Mungu anajua kila kitu. Na mwanamke anapo kuwa na damu anakuwa hana raghba ya kuingiliwa, basi kumuingilia wakati huo huenda kukamletea hali ya nafsi mbaya na chuki kwa jambo hilo.

2:228 – (1) Zingatia: Khabari ya eda ya mt’alaka limefasiriwa neno “Qurui” na wanazuoni wengi kuwa ni “Hedhi”. Na wamefasiri Shafii (na Malik) kuwa ni “T’ahara”. Khabari nyengine za eda zitakuja baadae. Sharia ya eda imekuja ili kuhakikisha kuwa ipo mimba au hapana, kwani hayo hayawezi kuhakikishwa ila baada ya kupita hedhi (au t’ahara) tatu, kwani mbegu za uzazi haziwezi kuishi baada ya hedhi tatu. Mwenye mimba kwa kawaida hatoki hedhi, na akitoka ni mara moja au sana mara mbili. Kwani hakika hapo ile mimba huwa imepevuka kwa muda huo hata kufikia kujaza eneo lote la tumbo la uzazi, na kwa hivyo ikazuia kuteremka damu ya mwezi. Hiyo ni kudra ya Mwenyezi Mungu katika kuumba kwake, na hayakuwa hayo yanajuulikana na Waarabu, na wala hayakuwa yajuulikaane na Nabii asiye jua kusoma. Lakini Mwenyezi Mungu alimteremshia Qur’ani, akamfunza yeye na akaufunza umma wake. Na sababu ya pili ya sharia ya eda ni kumpa fursa ya mt’alaka kurejea kwa mumewe baada ya kuwaza na kufikiri na kutua. Na hapo ni mume kusema: “Nimekurejea”. Lakini hii itahisabiwa ni moja katika t’alaka tatu.

(2) Mwenyezi Mungu amempa mwanamke haki kama zile zinazo mwajibikia yeye. Na

mwanamume amepewa cheo cha ulinzi na kuhifadhi. Na juu yake ni waajibu wa uadilifu. Uislamu ndio ulio mpa mwanamke haki ambazo hakupata kupewa na mila zote zilizo tangulia. Kwa Warumi mwanamke alikuwa ni kijikazi wa nyumba ya mumewe. Ana jukumu, lakini hana haki. Hali kadhaalika kwa Waajemi. (Na vivyo hivyo katika dini za Kiyahudi, Kikristo na Kibaniani. Paulo ameandika katika 1 Korintho: “Wanawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena bali watii, kama vile inenavyo torati nayo. Na wakitaka kujifunza neno lo lote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu kunena katika kanisa.” - 1 Korinth. 14.34-35. “Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume. Maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katoka katika mwanamume. Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume.” 1 Korinth. 11.7.9 “Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adamu hakudanganywa, mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa.” 1 Timotheo 2.11-14.

Na hapana popote katika Biblia panapo kataza Mayahudi au Wakristo kuoa wake wengi, isipo kuwa kauli moja tu ya Paulo inayo mpendekeza Askofu aoe mke asiye zidi mmoja. Kauli hiyo iko katika Waraka wa Kwanza wa Paulo kwa Timotheo 3.2: “Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, n.k.” Je, ni Uislamu au Ukristo ulio mweka chini mwanamke?)

2:229 - Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taa'la* ameifanyia sharia t'alaka, na akampa mwanamume kwanza uwezo wa kuacha. Baadhi ya watu wanadhani kuwa haya huleta madhara katika maisha na kusahilisha kuvunjika nyumba za watu. (a) Ama kupewa haki ya kuacha mwanamume kwa hakika hakupewa haki hiyo bila ya masharti yoyote. Katika masharti hayo aliyo wekewa ni:

KWANZA hana ruhusa kuacha ila t'alaka moja ya kuweza kurejea, yaani anakuwa na haki ya kumrejea mke kabla ya kwisha eda. Ama amrejee naye yu ndani ya eda au amwache, na hivyo tena ni dalili ya hadi ya kuchukiana, na hapana maisha ya mume na mke tena kuchukiana kumefika hadi hiyo.

PILI asimwache wakati wa hedhi, kwani wakati huo mwanamke huwa na hamaki, kwa hivyo huwa hapana utulivu. Na huenda hiyo hedhi ndiyo sababu ya hizo chuki zilizo zidi. Basi asiache mpaka mambo yawe yametua.

TATU asimwache naye yumo katika t'ahara aliyo kwisha muingilia, kwani hiyo yaweza kuonekana huko kuchukiana kunatokana na kutokuwa na raghba na mkewe. Basi mambo yakiwa hivi t'alaka inakuwa katika hali ya chuki iliyo na nguvu, na kukatika mapenzi ya daima.

2:233 - Qur'ani inawajibisha mama amnyonyeshe mwanawe na asinyonyeshwe na mwingine ila kwa dharura, kwani kunyonyesha yeye ni faida kwa mama na mtoto katika siha. Na kuachisha ziwa kuwe kwa taratibu, na yajuzu kabla ya kutimiza muda ikiwa siha ya mtoto inaruhusu hayo.

2:255 - Katika haya upo ushahidi wa kuonyesha ujuzi wa Mwenyezi Mungu wa daima, na Kusimamia kwake kusio koma kwa yote ya mbinguni na duniani. Pia pana ishara ya kuwa Mwenyezi Mungu hapitikiwi na vituko vinavyo zuka. Ilimu ya Sayansi imethibitisha kuwa kulala ni katika sifa ya wanyama na mimea iliyo hai. Ikiwa Mwenyezi Mungu halali basi Yeye ni hai kwa uhai ulio elekeana na dhati yake, lakini sio kama vilivyo hai vinginevyo.

2:260 - Ametaja Al Fakhri Al Razi na wengineo kuwa yapo maoni mengine juu ya tafsiri ya maneno haya matukufu. Nayo ni kuwa Ibrahim hakuwachinja wale ndege, wala hakuamrisha kuwachinja. Bali aliamrisha awakusanye kwa kuwazoeshwa kukaa naye. Kisha akawagawa akaweka juu ya kila kilima ndege mmoja. Kisha akawaita wakamjia. Na hii ni namna Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyo umba, ni kwa amri yake ya “Kuwa” basi huwa, kama alivyo waita wakaja.

2:265 - Neno la Qur’ani “ardhi iliyo nyanyuka” linaashiria yaliyo vumbuliwa na ilimu za sayansi za kisasa, kuwa maji ya chini yanakuwa yako mbali na mizizi. Kwa hivyo mizizi haozi na vijizizi vidogo vinapata kunyonya chakula kwa wasaa na pia kuvuta pumzi. Kwa hivyo mazao yanakuwa mema, kwa mvua ijayo au hata manyunyuni. (Nasi twajua mikarafuu au minazi ya bondeni haina maisha wala haistawi.)

2:266 - Ilimu ya kisasa inaeleza kuwa katika anga pepo kali hugongana zikatoka radi na umeme na mvua. Huenda ukatokea moto kwa umeme kwa kugongana mawingu, au pengine huweza kutokea vimondo kutokana na volkano (burkani) iliyo karibu ikateketeza miti na chochote kilicho katika sehemu hizo. Qur’ani inaashiria maana zote hizo.

2:275 - Riba iliyo tajwa katika Aya hii ni riba ya kijahiliya, nayo ni ziada juu ya deni kwa sababu ya kuakhirisha kulipa. Hii ni haramu, ikiwa kidogo au nyingi. Amesema Imam Ahmad: Haimfalii Muislamu kukanya haya. Kinyume cha hayo ni faida ya biashara, na hii inathibitishwa na hadithi ya Mtume s.a.w.: Ngano kwa ngano, kama ile ile, mkono kwa mkono. Shairi kwa shairi, kama ile ile, mkono kwa mkono. Dhahabu kwa dhahabu, kama ile ile, mkono kwa mkono. Fedha kwa fedha, kama ile ile, mkono kwa mkono. Na tende kwa tende, kama ile ile, mkono kwa mkono. Mwenye kuzidisha au kutaka kuzidisha basi amekula riba. Wanazuoni wamewafikiana kuwa ni haramu kuzidisha katika kubadilishana kitu cha jinsi moja, na wameruhusu kuzidisha ikiwa vitu vya jinsi mbali mbali. Lakini wameharimisha kuakhirisha katika vitu vya namna hii. Na wamekhitilafiana katika kukisia vitu vingine khitilafu kubwa. Katika rai iliyo karibu mno ni kukisia kama haya kila kinacho liwa kinacho weza kuwekwa kisiharibike. Ama riba ya kijahiliya hapana khitilafu yoyote -- mwenye kukanya basi ni kaafiri.

Riba ya kijahiliya humtia dhiki na kiwewe mwenye kula na mwenye kuliwa, kwa wasiwasi na kumshughulisha akili kwa mali aliyo kopesha au aliyo kopa. Mwenye kukopa ana dhiki na kushughulika akili yake hata hawezi kushughulikia kazi yake, na mwenye kukopesha anakuwa na hamu na khofu kuwa hatolipwa. Na baadhi ya madaktari wanaona kuzidi kwa maradhi ya “presha” na moyo ni kwa sababu ya kuzidi

riba. Na kuharimishwa riba na Qur'ani kunawafikiana na mafailasufi wa zamani, kama Aristotle alivyo sema kuwa uchumi wa riba si uchumi wa tabia, kwani pesa hazizai pesa. Wataalamu wa uchumi wamethibitisha kwamba njia za uchumi ni nne: Tatu katika hizo ni zenye kuzaa matunda, ama ya nne haizai kitu. Zenye kuzaa ni kibarua, tena inafuatia ufundi na ukulima na kujasirisha katika biashara, kwani katika hiyo ni kuhamisha bidhaa kutoka pahala zilipo undwa kuzipeleka pa kuzitumia, na hiyo kwa hakika imekuwa ni kuzalisha matunda. Ama njia ya nne ndiyo hiyo faida ya riba. Katika kukopesha hajitii mtu khasarani bali ni faida tu, na hapana kuzalisha matunda ila kwa kazi ya yule aliye kopeshwa. Faida yake ni kwa kiasi ya mkopo. Ikiwa sababu yenyewe ni mkopo mwenye kukopesha haingii khatarini kwa kuwa anayo dhamana.

2:282 - Aya hii inahakikisha misingi ya kuthibitisha. Inahakikisha msingi wa kuandikiana. Hukumu haiwi kwa chini kuliko mashahidi wawili walio wanaume waadilifu, au mwanamume mmoja na wanawake wawili. Na imelazimika mwandishi awe muadilifu, na wawepo mashahidi panapo kuwapo mafungamano. Lakini hapana lazima ya mashahidi ikiwa mua'mala wenyewe wa papo kwa papo, nipe nikupe, mkono kwa mkono. Pia aya inahakikisha kuwa mtu aliye pumbaa, au hawezi kujiendeshea mambo yake mtu mwenyewe, au mnyonge dhaifu, basi lazima awe na mtu kuwa ni wakili wake wa kumtendea badala yake. Na pindi ikiwa ni safarini na hapana mtu wa kuandika, basi yatosha kutoa kitu kiwe rahani akamate mwenye kukopesha.

3:123 - Badri ipo mwendo wa kiasi ya maili 120 kusini magharibi ya Madina. Mpambano hapo baina ya Waislamu na Makureshi ulikuwa siku ya Jumaane 17 Ramadhani mwaka wa pili wa Hijra (13 Machi 624 B.K.). Mtume s.a.w. na Masahaba wake walitoka Madina taarikh 8-9 ya Ramadhani mwaka wa pili wa Hijra (5 Machi 624 B.K.) Idadi ya wapiganaji wa Kiislamu katika vita hivi ilikuwa kiasi watu mia tatu au zaidi kidogo, na Washirikina walizidi mara tatu kuliko hao. Mwenyezi Mungu alitimiza ahadi yake katika vita hivi, Waumini wakashinda juu ya kuwa ni wachache, kwa kuwa Imani yao juu ya haki na uadilifu ilikuwa kubwa. Na kuungwa mkono na Mwenyezi Mungu pamoja na kuwa na moyo wenyewe kulikuwa ni sababu za ushindi kuliko wingi wa watu na ubora wa silaha. Ushindi huu ulio dhaahiri ukawa ndio sababu ya kuenea Neno la Imani na kutukuka likawa juu. Na hichi ni chanzo cha yaliyo kuja baadae, na kivuli cha Uislamu kikatanda Arabuni kote, na kisha kwengineko ulimwenguni.

3:190 - "Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi, na kukhitalifiana usiku na mchana ziko ishara kwa wenye akili" -

Aya hii ina ukweli unao onyeshea taadhima ya Muumba. Mbingu ni moja katika Ishara za Mwenyezi Mungu inayo tubainikia kwetu kwa miale ya jua inayo piga juu ya anga linalo izunguka dunia. Miale hii inapo angukia chembe chembe na vumbi vumbi jembamba liliopo angani humulika mianga hiyo na kutawanyika kila upande. Huu mwanga mweupe kwa hakika ni mkusanyiko wa rangi zote zionekanazo. Hizi chembe chembe za angani huzimeza baadhi ya hizo rangi.

Imedihiri kuwa rangi yenye kuenea zaidi ni rangi ya kibuluu. Na hii inazidi kuzagaa linapo kuwa jua liko utosini, na ubuluu wake unapungua kidogo kidogo mpaka jua

linapo kuwa upeo wa macho wakati wa magharibi au alfajiri. Wakati huo ile miale ya jua inakwenda masafa makubwa zaidi kabisa. Kwa hivyo zile chembe chembe za angani huzimeza rangi zote isipo kuwa rangi nyekundu.

Usafi wa maneno ni: mwangaza wa mchana unahitaji miale ya jua na kuwepo vumbi la kutosha katika anga. Dalili ya hayo ni yale yaliyo tokea mwaka 1944 mbingu ilipo ingia kiza ghafla kati ya mchana. Jinsi ya kiza mchana ukawa kama usiku. Kwa wakati mfupi yakawa hayo, kisha mbingu ikawa nyekundu, kisha kidogo kidogo ikawa rangi ya machungwa, na kisha ya manjano mpaka mbingu ikarejea rangi yake ya tabia, baada ya saa au zaidi.

Baadae ilibainika kuwa mambo hayo yalitokana na mripuko mbinguni likatokea jivu, likachukuliwa na upepo mbali mpaka Afrika ya kati na kaskazini, na kufika magharibi ya Asia. Huko ndiko ikaonekana hali hiyo katika pande za Syria. Maelezo yake ni kuwa vumbi lilioko hewani liliifunika nuru ya jua. Lilipo pungua jivu ulidhihiri mwangaza mwekundu na baadae wa manjano n.k.

Mwanaadamu akipaa angani katika chombo atapitia matabaka yanayo khitalifiana sifa. Ataiona mbingu inazidi ubuluu mpaka akifika kwenye anga la nje lisio kuwa na hayo mavumbi n.k. ataona mbingu yote ni kiza kitupu kama kwamba ni usiku juu ya kuwa jua lipo juu. Kwa ufupi ni kuwa zipo mbingu nyingi si moja ziliyo pandana tabaka kwa tabaka kama maqubba, zinazo khitalifiana katika sifa zake na rangi zake.

Haya ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliye takasika kuwa vyote viliomo mbinguni na ardhini vinamtukuza Yeye. Ama kukhitalifiana usiku na mchana, tumekwisha fahamu kuwa mwanga wa mchana unategemea miale ya jua kuanguka juu ya hili funiko la anga, lenye chembe chembe za vumbi kwa kiasi maalumu. Mwangaza huu ni mkali hata unaficha mwangaza unao toka kwenye nyota n.k. Ama wakati wa usiku mwangaza wa jua unapo fichika, inakuwa hapana katika anga isipo kuwa vumbi linalo tuzunguka na mianga dhafu ya nyota. Kupishana usiku na mchana ni kwa sababu ya kuzunguka dunia kwa nafsi yake wenyewe, na tafauti ya misimu na kurefuka na kufupika usiku na mchana ni kwa mzunguko wa hii dunia kulizunguka jua. Na katika hikima yake Mwenyezi Mungu na uwezo wake ni kuwa kubadilika usiku na mchana, na kubadilika misimu ya joto na baridi, ni kutengeneza hali ya hewa iwe wastani, yaani kati na kati, kwa kusilihi maisha ya vilivyo hai.

3:200 - Jee! Baada ya kuijua Qur'ani yamfalia Muislamu kusema kuwa dini ni kitu mbali na siyasa? Vipi uamrishe mema, ukataze maovu, uhukumu, ukatibiane mikataba na dola nyengine, ukusanye zaka na kuzigawa, upigane Jihadi, ulinde mipaka n.k., n.k. na uiepuke siyasa?

Amesema Prof. Khurshid Ahmad: “Uislamu si dini kwa maana ya ovyo ovyo kama lilivyo potoshwa neno hilo, yaani kuwa umemkhusu mtu maisha yake ya binafsi tu. Ni mwendo kaamili wa maisha, unao angalia kila midani ya uhai wa binaadamu. Uislamu ni uwongozi katika kila nyendo za maisha - za binafsi na za jamii, za kimwili na kiroho, za uchumi na siyasa, za sharia na mila, za taifa na za mataifa.” (Uislamu, Maana na Ujumbe wake uk. 37).

4:3 - Sharia ya Kiislamu si peke yake inayo ruhusu kuoa wake wengi, miongoni mwa sharia za dini za mbinguni. Sharia ya Taurati inamruhusu mwanamume kuoa idadi ya

wanawake atakao. Na imetaja kuwa Manabii walikuwa wakioa wake kwa makumi na makumi. Na Taurati ni katika Agano la Kale la Biblia ambalo linafuatwa pia na Wakristo katika mambo ambayo hayakukatazwa katika Injili au Barua za Mitume. Na hakika iliopo ni kuwa hapana popote katika Agano Jipya panapo pinga sharia hiyo ya kuruhusu kuoa wake zaidi ya mmoja.

Kanisa katika Karne za Kati liliruhusu hayo, na wafalme wa Ulaya wa Kikristo walio kuwa na wake wengi ni maarufu katika taarikh (historia).

Khitilafu iliopo ni kuwa Uislamu ndiyo dini ya kwanza kuweka idadi maalumu, isipindukiwe. Imeweka kiwango kwa mambo matatu.

* (Kwanza) wasipindukie hao wake kuliko wane.

* (Pili) asidhulumike mmoja katika hao wake,

* (Tatu) awe mtu anaweza kuwakimu hao wake.

Shuruti mbili za mwisho zimelazimu kila ndoa, ijapokuwa ni ya kwanza. Wanazuoni wa Kiislamu wa sharia na wanga khitalifiana wanakubaliana pamoja kuwa mume ambaye anajua kuwa hawezi kuwafanyia uadilifu wakeze ni haramu kwake kidini kuongeza wake. Ila uharamu huu ni wa kidini, watawala na mahakimu hawawezi kumingilia. Kwani uadilifu ni jambo la nafsi yake mtu, na dhamiri yake, na uwezo wa kutazama ni jambo la mnasaba halifungamani na mizani mojado. Ni yeye mwenyewe atakaye pata adhabu Siku ya Kiyama akikhalifu amri hiyo. Dhulma au kutokuweza kukimu kunategemea hali ya siku zijazo, na mikataba haifungamani na mambo ambayo huenda yakawa au yasiwe, bali ni juu ya yaliyoko, na ilivyo kuwa dhaalimu huenda akawa muadilifu, na asiye weza sasa hueza akaweza baadae, kwani mali huja na kuondoka, juu ya hivyo Uislamu unasema mwanamume akimdhulumu mkewe au akashindwa kumkimu, basi mwanamke anaweza kutaka kufarikishwa na mume huyo, lakini hazuiliki na kuandikiana mkataba akifanya hayo kwa radhi yake na khiari yake. Na Uislamu kwa kufungua mlango wa kuoa wake zaidi ya mmoja lakini kwa mikazo kama hivyo ilivyo elezwa imekuwa umepiga vita magonjwa ya kijamii:

* Kwanza - Huenda ikawa idadi ya wanaume wanao faa kuoa ikawa chini kuliko wanawake wanao faa kuelewa. Khasa huwa hayo baada ya vita. Imeonakana katika baadhi ya nchi za Ulaya imewahi kufika idadi ya wanawake kuwazidi wanaume baada ya vita kwa mara saba! Kwa hivyo ni hishima ya mwanamke katika hali kama hizo kuwa mke-mwenza kuliko kuwa akibahashika kama malaya, bila ya mume.

* Pili - Huenda kutokea baina ya mwanamume na mwanamke hali inayo walazimisha ama waingiane kiharamu au waoane kisharia. Ni maslaha kwa umma yawe hayo kwa mujibu wa sharia. Na ni bora kwa mwanamke kuwa mke kuliko kuwa hawara wa mwanamume huyu baada ya huyu. Ikiwa hii ni sura mbaya ya kuoa wake wengi, basi juu ya hivyo ni afadhali kuliko kuwa na mke mmoja. Kwani kuoa wake zaidi ya mmoja kama itavyo kuwa vibaya kunakinga shari kubwa zaidi kwa umma, nayo ni umalaya na maovu yanayo pandana nayo.

* Tatu - Mwanamke hakubali kuolewa na mume mwenye mke ila ikiwa ni kwa dharura iliyo kweli. Ikiwa mke wa kwanza atapata madhara kwa uke-wenza, basi huyu mwenzie atapata madhara makubwa zaidi kwa kuharimishwa mume kabisa, kwa kuwa ama ufe uke wake au apotee kwa wanaume majiani. Madhara makubwa hukingwa kwa madhara yaliyo akali.

* Nne - Imeonakana kuwa vijana wengi hawapendi kuoa, hata inakisiwa kuwa vijana

wanao oa kwa kulinganisha na wafaa kuoa hawazidi kuliko 60%. Na haya yanazidi kila mwaka. Kupinga khatari hii hapana ila kuruhusu kuoa wake wengi.

* Tano - Huenda mke akapata maradhi ambayo hayamruhusu kulala na mumewe, au huenda akawa tasa. Ni maslaha ya umma na maslaha ya binafsi kuoa mke mwengine. (Wakati huo huo ikawa kumpa talaka huyo mke ni madhara makubwa zaidi kwa mke na ukatili kwa mume kufanya.)

Kwa sababu kama hizi na nyenginezo Uislamu umeufungua mlango kwa shida na dhiki, na haukuufunga kabisa. Hivi sasa tunamwona Askofu Mkuu katika Uingereza anaona kuwa dawa ya pekee ya kuondoa uharibifu ulio uingilia ukoo wa Kiingereza ni kufungua mlango wa kuoa wake zaidi ya mmoja. Hakika Uislamu ni Sharia ya Mwenyezi Mungu ambaye anajua kila kitu. Kwani Yeye ndiye Mjuzi Mwenye hikima. (Haya tukijua kuwa dini ya Kikristo haikatazi kuoa wake wengi. Ni sharia zilizo tungwa na makanisa ya Kizungu tu kwa kufuata mila zao ndizo zinazo lazimisha kuoa mke mmoja. Basi hiyo ni mila ya Wazungu, wala si sharia ya dini yoyote duniani. Bali Uislamu ndiyo Dini pekee katika dini zote iliyo wekea kiwango, na kudhibiti idadi ya wanawake kuoa, kwa maslaha ya Umma.)

4:13 - Mpango wa mirathi uliyo bainishwa na Qur'ani Tukufu ni mpango wa uadilifu na haki kuliko kanuni zote za mirathi nyenginezo duniani. Na haya wameyakiri wataalamu wa sharia wote wa Ulaya. Na huu ni mmoja katika ushahidi wa kuwa Qur'ani inatokana na Mwenyezi Mungu, kwani haya au yaliyo karibia haya hayakuwa yakijuulikana kwa Waajemi wala kwa Warumi wala katika sharia zozote za kabla ya Uislamu. Na sharia hii ya Kiislamu imefuata mipango hii ya uadilifu:

* Kwanza - Umefanywa urithi kwa mujibu apendavyo Mwenyezi Mungu, sivyo apendavyo mwenye mali, bila ya kupuuza kabisa mapenzi yake huyo. Amepewa huyo ruhusa ya kufanya wasia kwa thuluthi ya mali kwa ajili ya mambo mema, kama kutimiza kasoro katika wajibu wake wa dini, kama Zaka ambazo alikuwa hakuzitoa, au kuwajaalia kitu wahitaji alio khusiana nao kwa ujamaa au mapenzi nao hawastahiki urithi. Na amezuiliwa kufanya wasia ikiwa hayo yatapelekea maasi au yatachochea kuendelea maasia. Na thuluthi mbili zilizo baki baada ya wasia, au mali yote ikiwa hapana wasia, Mwenyezi Mungu Mtunga sharia, amejipa Yeye kuzigawa kwa haki.

* Pili - Katika kuchukua madaraka ya ugawaji tirka, Mwenyezi Mungu Aliye takasika, amempa aliye karibu zaidi kuliko mwenginewe, bila ya kuzingatia ukubwa au udogo. Kwa hivyo ndio ikawa watoto wana sehemu kubwa zaidi katika mirathi, kwani wao ndio kiendelezo cha yule maiti, na pia kuwa wao aghlabu ni wanyonge. Juu ya hivyo hawakukoseshwa, bali wameshirikiana nao, mama na bibi, baba na babu, ijapokuwa wanachukua akalli kuliko watoto.

* Tatu - Yaonekana kuwa mirathi ni kwa kadri ya haja. Kwa hivyo sehemu ya watoto ni kubwa kwa sababu haja yao ni kubwa zaidi, na wao ndio wanayakabili maisha, na kina baba na mama wanayapa mgongo maisha. Ama zingatia la haja ndilo lililo pelekea kuwa fungu la mwanamke liwe nusu ya fungu la mwanamume katika aghlabu ya hali za mirathi. Haya ni kwa kuwa mwanamume inambdi zaidi kukabili matumizi, kwa kuwa yeye anatakikana awalishe watoto na awatazame, amtumilie mwanamke. Maumbile ya kibinaadamu yamemfanya mwanamke ndiye asimamie kazi za nyumbani na kulea watoto, kuangalia raha zao, na mwanmume awe ni wa kuhangaika nje kiuchumi alete

fedha za kutumia nyumba nzima. Kumpa kila mmoja kwa kadri ya haja ndio uadilifu. Kuweka sawa kwa wenye haja mbali mbali ni udhalimu.

* Nne - Sharia ya Kiislamu katika kugawa kwake tirka ya maiti inakusudia kugawa sio kurundika. Kwa hivyo haikufanya urithi wende kwa mtoto mkubwa peke yake, wala haikuwapa wanaume tu na kuwachilia mbali wanawake, wala watoto wakaachwa wazazi. Wala hawakukoseshwa wasio kuwa katika uti wa nasaba, kama ndugu, na maami, na banu-ami n.k. Urithi unaendelea mpaka kwa wanao karibia ukoo, lakini aliye karibu hufadhilika zaidi. Na shida kutokea kuwa mrithi ni mmoja tu.

* Tano - Mwanamke hakoseshwi kurithi, kama ilivyo kuwa ada ya Waarabu. Hivi ni kumhishimu mwanamke na kumpa haki yake. Na juu ya haya Uislamu hauzuii kurithi ujamaa wa mwanamke, bali hurithi jamaa walio kuwa upande wake, kama wanavyo rithi jamaa upande wa baba. Makaka na madada kwa upande wa mama wanachukua pale wanapo chukua ndugu wa baba na mama, bali katika hali nyengine wanachukua watoto wa kwa mama na kuchukua ndugu wanaume na wanawake. Na haya bila ya shaka ni kuutukuza umama, na kuutambua ukaribu wake. Haya hayakuwa yakijuulikana kabla yake, walakini hii ni Sharia ya Mwenyezi Mungu aliye Mjuzi na Mwenye hikima.

4:22 - Waarabu katika zama za ujahili walikuwa na ada zisio mpa heshima mwanamke, bali zikimdhulumu sana, na zikikata makhusiano mema katika ukoo. Ilikuwa mtu akifa baba yake na akawa na wake wasio kuwa mama yake mzazi, akilazimishwa kuwaoa, au akiwarithi wake za baba yake bila ya ndoa mpya. Na ilikuwa mtu akimwacha mke basi humpokonya kwa dhulma na uadui mahari yote aliyo mpa. Na walikuwapo walio kuwa wakimzuia huyo mt'laka asiolewe na mtu mwengine, kwa jeuri na inda. Ukaja Uislamu, ukamlinda mwanamke na dhulma hii iliyo wazi, ukakataza kurithiwa mke, na kumpokonya mahari yake hata chembe, ijapo kuwa ni mali mengi, na ukakataza kumzuia mt'alaka asiolewe, au kumkera ili apate kutaka yeye mke t'alaka kwa kutoa mali. Na katika mtindo wao Waarabu wa jahiliya ilikuwa yafaa mtu kumwoa aliye kuwa mke wa baba yake na akafarikiana naye kwa t'alaka au mfano wake. Uislamu ukakataza hayo, na ukauwita mtindo huo ni uchafu, kwa sababu ni jambo baya analo lichukia Mwenyezi Mungu na kila mwenye akili sawa. Huo ndio uadilifu wa Mwenyezi Mungu.

4:23 - Ni Sharia ya Kiislamu pekee iliyo harimisha kwa sababu ya kunyonyesha. Anaye nyonya anakula kutokana na mwili wa mnyonyeshaji kama anavyo kula kutokana na mama yake ndani ya tumbo lake. Wote hao wawili wanakuwa ni sehemu yake huyo mtoto. Hapana khitilafu baina ya kukua ndani ya chumba na ndani ya tumbo. Na katika kuharimisha kwa kunyonyesha ni kumtukuza mnyonyeshaji, kwani anakuwa kama mama. Na haya ni kuzidi kushajiisha kunyonyesha kimaumbile, sio kwa chupa, kwa watoto wachanga.

4:56 - Qur'an Tukufu imeitangulia sayansi ya kisasa, ikathibitisha kuwa katika ngozi mishipa ya kuhisi, Navo, imetanda kama wavu, na hiyo hupokea mishipa yote ya kuhisi machungu, joto na baridi na mengineyo. Na hayo hayakujuulikana ila hivi karibuni.

4:92 - “Kuulipa” kwa kuwa utumwa ni amana ya mtu, na kumkomboa mtumwa ni kumhuisha mtu. Akiuliwa Muumini kwa kukosea, na mwenye kuuwa akakomboa shingo ya Muumini basi huyo amehuisha na kuulipa umma.

4:102 - “Laahiq” ni anaye sali na Imam mwanzo wa Sala na akalazimika kusali iliyo baki peke yake, na “Masbuuq” anaye iwahi sehemu ya mwisho ya Sala ya Jamaa, kisha akatimiza sehemu aliyo ikosa peke yake.

4:176 - Na Sunna (Mafunzo ya Mtume) imebainisha kuwa wakizidi kuliko ndugu wa kike wawili, pamoja na Aya ya mirathi iliyo tajwa, kuwa wakizidi kuliko binti wawili, watachukua thuluthi mbili. Ni bora kuwa zaidi kuliko ndugu wawili wa kike, kwa sababu mabinti ni karibu zaidi kwa maiti.

Tuzingatie kuwa kwa mujibu wa kanuni za Kizungu za kurithi, ambazo zimetokana na kanuni ya Kirumi, ndugu wanaume wala wa kike wala watoto wao hawarithi. Na juu ya hivyo mwenye mali anayo ruhusa kumkata yeyote asipate urithi wake. Uislamu umekataza haya. Warithi lazima wapate urithi wao, ila mtu anayo haki ya kuandika wasia kujihukumia kisicho zidi thuluthi moja ya mali yake. (W.H. Ingrams katika kitabu chake Zanzibar Its History and Its People ameandika: “Hakika Sharia Takatifu yaonekana kuwa ni ya haki zaidi sana kuliko hata mpango wa Kiingereza wa kugawanya mali. Katika Zanzibar [na bila ya shaka katika Waislamu wote] hapana mwendo wa kuwa mtu “kukatwa urithi akabakishwa na shilingi moja tu”; vyo vyote vile, ni sehemu ndogo tu ndiyo inaweza kuandikiwa wasia, na yaliyo baki lazima yagawiwe kwa warithi kwa mujibu wa kiwango maalumu.”)

5:2 - Mwenye kuhiji akisha “harimiya” (yaani kunuia kuhiji) huwa haramu kwake baadhi ya mambo, kama kuvaa nguo iliyo shonwa, kukata nywele, kuwinda, n.k. mpaka amalize “Ihram” nako ndio kwisha ibada ya Hija.

5:3 - Hafi mnyama wenyewe ila kwa maradhi, na hayo maradhi humdhuru mwanaadamu akila nyama yake, na huenda maradhi mengine yakawa ya kuambukiza. Katika damu vimo vijidudu vya maradhi. Ama katika nyama ya nguruwe mna vitu kadhaa wa kadhaa vya kumdhuru mtu. Na vilivyo chinjwa kwa jina la asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na walio chinjiwa masanamu au mashetani, hayo ni mambo ya ibada potovu. Na vilivyo nyongeka, na vilivyo anguka, na kupigwa pembe ni sawa na mfu, au mzoga, kwa kuwa vimekufa kwa vifo vibaya, na khasa kwa kuwa damu yake haikutoka imevilia humo humo.

5:6 - T’ahara (Usafi) wa Kiislamu una maana mbili: Moja ni kumwelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu moyoni kwa kujiweka tayari kwa hayo, na kufunga azimio kusimama mbele yake na hali ni mwenye nafsi iliyo t’aaahiri, na moyo ulio safi kabisa kwake Yeye tu. Pili ni unadhifu wa dhaahiri kwa udhu. Na katika hayo ni kuvikosha viungo vyote vinavyo weza kuchafuka. Na udhu ni jambo la kufanywa mara kwa mara, na huweza kufika hata kutwa mara tano. Pia kuna kukoga unapo ingiliana na mke, na wakati wa damu ya mwezi na uzazi. Udhu na kukoga ni kuondoa takataka zenye vijidudu vya maradhi, na pia huleta uchangamfu kwa kuisimua damu ya kwenye ngozi, na kupoza

mishipa. Na kwa hivyo Mtume s.a.w. aliusia: “Ukihamaki tawadha”.

5:8 - Uislamu unalingania uadilifu moja kwa moja, sawa kwa rafiki na adui. Haifai chuki ikakupelekea kudhulumu. Na hayo unapo amiliana na watu, na kuamiliana baina ya dola ya Kiislamu na dola nyenginezo. Na kumfanyia uadilifu adui kunaambiwa na Qur’ani kuwa ni karibu zaidi na uchamngu na usafi wa kidini. Lau kuwa wasia huu ungesi tumiwa katika sharia za baina ya madola basi pasingeli kuwapa vita. Kama kila dini ina kitambulisho chake na alama, basi kitambulisho cha Uislamu ni Dini ya Mungu Mmoja na Uadilifu.

5:32 - Maneno haya yanaonyesha kuwa kumfanyia uadui mtu mmoja ni kuwafanyia jamii ya watu, na kulipa kisasi ndio kuhuisha jamii. Katika Sharia ya Kiislamu kisasi ni haki ya waliy-amri, yaani aliye mkuhusu maiti. Akipenda atasamehe na achukue fidiya, na akipenda atataka kisasi na akitimize. Naye anapo samehe anayo haki ya kumfedhehesha mkosefu akiwa amekithiri uwovu wake na uharibifu.

5:34 - Katika hukumu hii inabainishwa kuwa Sharia inaangalia ukhalifu unao athiri jamii, na kwa hivyo adhabu yake ni kali kwa kuwafikiana na kitisho chake kwa wapendao amani. Mazingatio hapa si kwa mujibu wa kile kitendo cha ukhalifu, bali kwa mujibu wa kiasi ya kitisho na fazaa inayo letwa na hicho kitendo.

5:49 - Maneno haya yanatukuza Sharia ya Kiislamu katika kuwahukumu watu. Kwanza inatukuka kwa kuwa ni hukumu ya uadilifu na haifuati mipango ya watu ijapo kuwa ni mipotovu, bali inahukumu juu ya hiyo mipango ya watu kwa kheri na shari. Pili Kanuni huwa katika dola ni moja tu kwa watu wote na mat’abaka yote.

5:89 - Katika hukumu ya yamini pana mawili yafaa tuyazingatie. Kwanza: Uislamu umeraghibisha sana kukomboa watumwa. Sababu nyingi zinazo wajibisha hayo. Kafara nyingi za dhambi zinahitaji kukomboa. Kafara ya kula mchana Ramadhani yahitaji ukombozi, n.k. Na katika hayo yanaonyesha Uislamu unachukia utumwa. Uislamu uliukiri utumwa kwa kuwa maadui wao walikuwa wakiwatia utumwani Waislamu, basi na Uislamu ukaruhusu kuwatendea wao vivyo hivyo. Pili: Uislamu unakazania kulisha masikini kila ikipatikana fursa.

5:90 - Kuagua kwa mishale: ilikuwa ikiandikwa juu ya vijiti, kimoja kiliandikwa: “Mola wangu Mlezi kaniamuru”, na kingine: “Mola wangu Mlezi kanikataza”, na kingine hakikuandikwa kitu. Hutiwa vijiti hivyo katika mfuko kisha huchanganywa, na kohani hutia mkono wake akachomoa kimojapo, na akamjuvya mwenye kuuliza lilio aguliwa.

5:91 - Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliye takasika ametaja mambo mane yaliyo pelekea kuharimishwa ulevi na kamari:

* La Kwanza - Kuwa nafsi yake ni uchafu na uovu, kwani hayumkiniki kusifika kuwa ni mambo mazuri, kwa kuwa madhara yake yanaonekana wazi. Katika ulevi kuna uharibifu wa akili, na katika kamari ni kupoteza mali, na kwa yote mawili hayo upo uharibifu wa moyo. Na Shetani ndiye mwenye kuyapamba hayo.

* La pili - Hayo hueneza uadui na chuki. Kamari humalizikia ugomvi, na kama haifikii hayo basi huleta chuki na bughdha. Na ulevi ndio Mama wa Maasi. Utamwona mtu mwenye adabu zake mpole, akisha kunywa hugeuka m nyama mwitu, akatenda mambo ya ukhalifu, kwani ulevi huidhoofisha sauti ya utu inayo mkataza mwanaadamu kutenda maovu. Utamwona mtu anajizua kufanya kitendo kiovu, lakini akisha kunywa ulevi, au akavuta bangi, japo kidogo, huiendea shari bila ya kujali. Basi si kama ulevi unaharibu akili tu, bali unalaza dhamiri ya mtu. Anakuwa hana junaha.

* La tatu: Ni kuwa kamari na ulevi huuwa moyo. Mtu huwa hamkumbuki Mwenyezi Mungu, na kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndiko kunako huisha nyoyo.

* Lane: Maasi hayo yanamzuilia mtu na Sala. Kamari na ulevi humsahaulisha Muumini na Sala zake, na akiwa anasali hatimizi nguzo zake kama zitakikanavyo. Basi inakuwa Sala zake ni kuinama na kuinuka bila ya kufuatana na moyo. Kwa hivyo basi imethibiti kuwa kuharimishwa mvinyo, pombe, tembo, bangi n.k. si kwa sababu ya kulevywa kwake tu, bali ni kwa kumziba mtu fahamu zake, kumgubika asitambue atendalo. Na kwa hivyo ndio imepokewa kuwa kinacho levya kwa wingi wake, basi hata kidogo chake ni haramu, kwani hicho kidogo nacho kinapumbaza akili. Na juu ya haya pana madhara ya mwili kama madaktari walivyo thibitisha.

Kwa hivyo ulevi hata kidogo ni haramu. Mwenyezi Mungu Subhanahu ametaja sababu mbili za kuharimisha ulevi, na udaktari umezidisha kuwa ulevi kidogo haupotezi akili, lakini huzidisha uchangamfu au husabibisha hali ya huzuni na kuona dhiki ya moyo. Na katika hali zote mbili anakuwa mtu amepungukiwa na ukamilifu wa akili yake kubeba jukumu, na kwa hivyo hutenda vitendo ambavyo kwa dhahiri ni sawa kumbe ni madhara. Ama kuuzoea ulevi hudhuru maini, matumbo, na mishipa ya akili na hisiya, na hurithisha madhara mpaka kwa vizazi.

5:103 - Wakati wa Jahiliya, kabla ya Uislamu, Waarabu wakijiharimishia wenyewe asiyo yaharimisha Mwenyezi Mungu. Katika hizo ni kuwa:-

1. Ngamia akizaa mara tano na mtoto wa mwisho akawa dume, basi wakimpasua sikio lake na wakaharimisha kumpanda, na akawa haijuzu kumfukuza kwenye kunywa maji au kula machunga. Na wakimwita: “Bahira”, yaani aliyeapasuliwa sikio.

2. Ilikuwa mtu husema: Nikirejea safarini, au nikipona maradhi yangu, basi ngamia wangu ni “Saiba”, yaani aliye achwa, na anakuwa kama “Bahira”.

3. Na walikuwa kondoo akizaa jike humfanya huyo mtoto ni wao, na akizaa dume humfanya ni wa miungu yao; na akizaa dume na jike basi hawamtoi mhanga huyo dume tena kwa miungu yao, na humwita huyo kondoo jike: “Wa’sila”, yaani amemuwasilia nduguye dume.

4. Na pia walikuwa akitokana na fahali mizao kumi basi husema mgongo wake umehamika, yaani umehifadhika, na wakamwita “Hami”. Huwa basi hapandwi, wala hatwikiwi mizigo.

6:1- Aya hii tukufu ni ishara ya ubora wa kuumba, na ubora wa kuumba unaonyesha Umoja na Upweke wa Mwenye kuumba na utukufu wake. Kwani mbingu na nyota zake, na sayari zake, na jua, na mwezi - vyote hivyo ni ushahidi wa Umoja wake. Na ardhi na viliomo ndani yake, navyo ni wanyama, mimea na visio na uhai, na milima na mabonde, na rutuba na ukame, na viliomo chini ya ardhi maadeni magumu na

yanayo tiririka, na bahari na viliomo ndani yake kama lulu na vilio hai - vyote hivyo vinaonyesha Umoja wa Mwenye kuumba. Na giza la kila namna, kama giza la jabali, na bahari, na mapango, na ukungu ulio funga moja kwa moja hata mtu akiutoa mkono wake anakaribia kuwa asiouone - pia vyote hivyo vinaonyesha ujuzi usio kuwa na mfano, wa kuanzisha kuumba, wa Mwenyezi Mungu Aliye viumba. Hali kadhaalika nuru, na sababu zake mbali mbali, kama nuru ya jua, na mwangaza wa mwezi, na mwangaza wa nyota, vyote hivyo vinaonyesha uanzishaji wa Mwenyezi Mungu wa kuumba bila ya kiigizo.

6:9 - Kauli hii inaashiria maana ambayo wenye ilimu za kisasa wanaitaja. Wenye ilimu za mambo ya kiroho wanasema kuwa roho zina mwili khafifu, mwembamba na mwepesi, mfano wa ng'amba. Nazo hazidhihiri wala hazionekani. Na hayumkiniki kuonekana roho ila zikivaa huo mwili. Na Malaika hawana kiwiliwili. Katika viumbe vyote vya kiroho Malaika ndio khafifu kabisa kushinda vyote. Na hayumkiniki kuonekana ila kwa sura ya mwili. Na huu mwili ndio unakuwa kama mwanaadamu.

6:59 - Kauli hii inafahamisha kuwa kujua mambo ya ghaibu kuko kwa Mwenyezi Mungu, na funguo za hayo ziko kwake tu. Na mambo ya ghaibu ni mafungu mawili: Ghaibu *Mut'laq* ambayo hayumkini kutambulikana na akili, kama mambo yatakayo mfikia mtu katika mustakbali. Na Ghaibu *Nisbiy* hizi ni siri za ulimwengu na viliomo ndani yake, na kuweza kuvitumia kwa maslaha ya watu. Ujuzi wa hayo huweza kughibu kwa vizazi kadhaa, kisha ukadhihiri.. Na funguo ya hizi pia ziko kwa Mwenyezi Mungu, humwezesha amtakaye katika waja wake wale wanao zama kuusoma ulimwengu. Na katika hayo ni haya ya uvumbuzi ambao tunauona anao ufikilia mwanaadamu kwa kuwezesha na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

6:95 - Imeunganishwa Aya hii ya kupasua mbegu na kokwa, na Aya ya kupambazua asubuhi ambayo inaashiria kuwepo mwangaza, na kiza, na ya kwamba mwangaza umeshikamana kwa nguvu na kukua kwa mimea na miti. Hayo ni kwa kuwa mbegu na kokwa baada ya kuchipua zinahitajia chakula. Na chakula hichi kinatokana na mbolea maalumu kutokana na ardhi, na pia kutokana na mwangaza wa jua. Kwa hivyo mizizi yao inakwenda chini kutafuta chakula cha ardhi, na vigogo vyake na matawi inapata chakula kutokana na mwako wa jua ambalo ndilo linachomoza asubuhi.

6:99 - Aya hii inafahamisha maana kwa ilimu ya sayansi, nayo ni kuwa maji husaidia mimea kuchipua. Mbegu iliyo kaa tu haitaharaki husisimka kwa kupata maji ikaanza kumea, ikafanya kazi yake ya uhai. Mimea tena hukua na kutoa majani yenye rangi ya kijani, nayo ni madda inayo itwa "Chlorophyl". Hiyo Klorofil ni lazima kuwepo kwa ajili ya kujenga chakula kwa msaada wa mwangaza wa jua, na kuweza kuukuza mmea na kutoa matunda na mbegu nyengine.

6:125 - Masomo ya ilimu za sayansi yamethibitisha kuwa mwanaadamu kila akipanda juu kunadhoofika kuvuta pumzi kwake kwa pua. Mpaka akifika mnyanyuka wa futi 12,000 huwa hawezi kuvuta kwa pua, na huvuta pumzi kwa mdomo. Na hivyo huvuta kwa shida, na akifanya juhudi yoyote ya nguvu huzidi taabu ya kuvuta pumzi. Na hata

kusema humletea shida katika pumzi.

7:54 - Aya hii tukufu imekusanya maana tatu:

* Ya kwanza ni kuwa mbingu na ardhi ameziumba Mwenyezi Mungu Mtukufu mnamo siku sita. Na hizi siku sio muradi wake hizi tuzionazo sasa, na tunazo zihisabu. Bali muradi wake ni kubadilika hali, baina ya giza totoro, na giza-giza la alfajiri, na mpambazuko wa asubuhi, na mchana, na adhuhuri, na jioni. Na haya yamekusanya hali sita zinazo badilika. Na giza-giza la magharibi linakitangulia kiza cha usiku.

Na hizo hali sita au vipindi sita, ambavyo vimeitwa “siku” ndivyo wanavyo vitaja wanachuoni wa sayansi, navyo ni: Kipindi cha “Ether”, kilicho elezwa katika Surat Ad-dukhan ya 44 ya kuwa ni moshi. Kisha kutokana na hiyo “Ether” yakatokea majua, ambayo moja lake ni hili jua letu. Kisha kutokana na jua zikawa sayari, na miongoni mwa sayari hizo ni hii dunia yetu. Tena katika ardhi zikawamo maadini mbali mbali. Tena ndio kikawa kipindi cha Ardhi, na baadae ukatokea uhai juu yake.

* Maana ya pili ya Aya hii ni kuwa kila kiliomo ulimwenguni kimo chini ya ufalme wa Mwenyezi Mungu peke yake, wala hapana ufalme usipo kuwa wake Yeye. Na nguvu zozote anazo pewa mtu hatoweza kuuendesha ulimwengu atakavyo. Ukomo wa uwezo wake ni kunufaika na vilivyo umbwa na akajua baadhi ya siri ziliomo ulimwenguni ambazo zilikuwa zimefichika. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu pekee ndiye aliye tuwa na kutawala juu ya A’rshi iliyo juu ya vyote vilivyo umbwa, na kwamba nyota na vitu vyote haviendi ila kwa amri yake peke yake.

* Maana ya tatu ni kuwa kupishana usiku na mchana kumetokea baada ya kwisha umbwa ardhi na mbingu. Basi hizo ni hali zenye kukhusika na asli ya uumbaji wa dunia, na makhusiano ya baina mbingu na ardhi na kuzunguka kwao na Mwenyewe Subhana Mwenye kuumiliki ufalme na utukufu na ukarimu.

7:65 - ‘Aad ni katika kabila yenye nguvu katika matumbo ya taifa la Sam, na ni katika mat’abaka ya kwanza katika Waarabu wa jangwani. Ama makaazi yao yalikuwa katika Al-ah’qaaf iliyo tajwa katika Kitabu kitukufu katika Sura ya Al-ah’qaaf Aya 21.

Wamewafikiana wanachuoni wa Kiislamu wa kutegemewa kuwa hiyo Ah’qaaf ipo katika nchi ya Yaman, ijapo kuwa wamekhitalifiana kidogo wapi khasa pahala penyewe. Kwa mujibu wa Yaaqut Al-h’amawy ni bonde baina ya Oman na nchi ya Mahara. Na kwa mujibu wa Is-haaq akimnukulu Ibn Abbas na Ibn Khaldun ni sehemu ya mchanga baina ya Oman na Hadhramaut. Kwa mujibu wa Qutaada ni sehemu ya mchanga karibu na bahari katika Shajar katika nchi ya Yaman. Na yafaa kutaja kuwa nchi ya ‘Aad kwa mujibu wa baadhi ya Wamagharibi wa zamani ipo pande za juu za Hijaz katika jimbo la Husmaa, na karibu na makaazi ya Thamud. Vyo vyote ilivyo si mbali kuwa hao kaumu ya ‘Aad walisafiri wakahamia jimbo hili wakati mmoja wapo.

7:73 - Thamud ni kabila ya Kiarabu iliyo kuwa Al Hijr, baina ya Hijaz na Sham karibu na Wadi Alquraa.

7:150 - Haarun amemwita Musa kwa kumnasibisha na mama yao, ijapo kuwa hao walikuwa ndugu khalisa, wa baba na mama, kwa sababu huyo mama alikuwa Muumini. Kumtaja yeye ni kuzidi kukumbusha mapenzi.

7:172 - Katika Aya hii inaonyesha kuwa watoto asili yake wanatoka kwenye uti wa mgongo. Na ilimu ya kisasa imethibitisha kuwa kokwa za khaswa zinakuwa katika sehemu ya mgongo chini ya mafigo. Na zinakaa hapa mpaka katika miezi ya mwisho ya mimba ndio huteremka pale pahali pake pa kawaida panapo onekana. Na pengine hata hivyo huchelewa kuteremka hata baada ya mtoto kuzaliwa. Kadhaalika mayai ya mwanamke yanafanyika chini ya figo khasa, kisha ndio huteremka pahala pake karibu na tumbo la uzazi.

8:7 - Aya hizi tukufu zinatoa sura ya yanayo pita katika nafsi wakati wa vita, nako ni kutamani kukutana na maadui wachache na kuchukia kukutana na wengi, na kupenda kuteka mali na ngawira; na ilhali Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka kuitukuza Dini na ishinde Haki na wang'oke makafiri.

8:9 - Walipo jua wapiganaji Waumini kuwa hapana njia ya kuepukana na vita wakaomba msaada kwa Mwenyezi Mungu, naye Mwenyezi Mungu Mtukufu akawaitikia, na akawaunga mkono kwa Malaika elfu walio fuatana. Yaani alianza kwa kupeleka msaada kwa vikosi vilivyo fuatana ili iwe wepesi kwa kila kikosi kuelekea pahala pake katika vita pasiwepo kukaa bure au kupigana makumbo. Na ifikapo misaada ya majeshi ya vita roho hufurahi na moyo huingia nguvu. Na hayo ndiyo aliyo yakusudia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kauli yake: “Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara na ili nyoyo zenu zituwe.” Na ushindi daima unatokana na Mwenyezi Mungu.

8:11 - Aya hii inaashiria fadhila ya Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya wapiganaji Waumini kwa kupatikana hali ya amani kwa kupumzika kwa usingizi, na kuteremka mvua kwa kujitahirisha na kukoga, na kushikamana mchanga kwa kuwepo maji, basi nyayo zikasimama imara. Inajuulikana kuwa mchanga laini unawaletea taabu wapiganaji na unakuwa pingamizi katika kwenda huku na huko ambako ni katika dharura za vita muhimu. Na aya ya pili inaeleza maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwaambia Malaika wawathibitisha Waumini na watie khofu katika nyoyo za makafiri. Na ni maarufu kuwa khofu ikiwatawala askari katika midani huwaletea kuemewa. Na katika Aya hii tukufu panaashiriwa pahali pa kupiga napo ni juu ya shingo na kuvikata vidole vinavyo kamata silaha mkononi.

8:57 - Katika Aya tukufu hizi tunahadharishwa na wale wanao toa ahadi na kisha wakazivunja. Hawa yafaa wapewe adhabu ya kutia mfano kwao na kwa walio nyuma yao. Na katika Aya hii unabainishwa umuhimu wa kuvuruga askari wa adui walio nyuma. Hizi ni mbinu za vita za kisasa, kwani kuzua vurugo katika askari wa nyuma hutosha kuleta fujo na kupelekea jeshi kutawanya askari wake kulinda mgongo wake, na kwa hivyo zinavunjika nguvu zake.

Juu ya hivyo katika sehemu za nyuma katika midani ndio huwapo mambo yaliyo khusu idara ya jeshi ambayo juu yake ndio jeshi linategemea kwa msaada. Ukileta vurugu hapa hupelekea kukosekana nidhamu yote ya jeshi, na kwa hivyo ndio huleta kuemewa na kushindwa.

8:60 - Katika Aya hii tukufu pana kuhimizwa na kuamrisha kujitayarisha kwa ajili

ya kupambana na adui. Kwani vita, zamani na sasa, ni jambo la khatari na muhimu kabisa. Juu yake inategemea kheri na shari, kufa kupona kwa umati na umati. Basi yapasa kujitayarisha, kujizatiti, na kujitengeneza kwa jiha mbali mbali za vifaa na silaha na zana. Kuingia vitani bila ya kujipatia zana zote na kujitayarisha ni kutafuta kushindwa. Na tunaona hivi sasa madola yanavyo jiandaa wakati wa amani na vita, na yanavyo jenga siasa zao na mipango yao na wanavyo kusanya uwezekano wao wote ili wapate ushindi katika vita. Na vita sasa havimsazi mtu. Wanashiriki katika vita wanajeshi na raia. Kwa hivyo ndio inapasa zaidi kujitengeneza kila mmoja wao kwa matengenezo ya kuwakusanya na kuwaweka tayari wote ili upatikane ushindi.

8:61 - Huu ni msingi mkuu katika misingi ya Uislamu, Dini ya Salama. Na leo tunasikia kila dola duniani ina nadi Usalama, na kwa hivyo ukaundwa Umoja wa Mataifa.

9:25 - Vita vya Hunayni walipigana Waislamu na kabila mbili za Thaqiif na Hawaazin. Jeshi la Waislamu lilifika kiasi ya watu elfu kumi na mbili, na makafiri walikuwa elfu nne. Nao walipigana kwa ukali kwa kuwa ilikuwa wakishindwa wao basi ibada ya masanamu itatoweka kabisa kwa Waarabu, kwani Makka ilikuwa ndio kwanza kwisha tekwa. Majeshi mawili yakapambana, Waumini kwa wingi wao, nao uliwapandisha kichwa; na wale makafiri na uchache wao wakali. Kwanza makafiri wakashinda kwa kuwa Waislamu walighurika kwa wingi wao wakajiona. Lakini mwisho vita vikaishia kwa kushinda Waumini. Funzo la hapa ni kuwa wingi sio unao pelekea ushindi, lakini nguvu za kimoyo na imani.

9:29 - “Jizya” ni katika kipato muhimu katika madukhuli ya serikali ya Kiislamu. Kodi hii ilikuwa baina ya Dirham 8 na 40. Kila mtu mmoja katika Mayahudi na Wakristo na walio kuwa kama wao akitozwa Dirham 12. Akilazimishwa kulipa mwanamume aliye kwisha baalighi, na mzima wa mwili na akili, na kwa sharti awe na mali ya kuweza kutoa. Wanawake na watoto walisamehewa, na vile vile vizee. Kwa sababu hao hawapigwi vita. Wala hawatozwi vipofu na wasio jiweza, ila wakiwa matajiri. Kadhaalika hawatozwi mafakiri na masikini na watumwa. Wala hawakutakiwa kutoa mamonaki, yaani mapadri wanao jitenga na watu.

Na asli ya kutozwa Jizya ni ulinzi wa wasio kuwa Waislamu. Kwa sababu Ahli Lkitaab, Watu wa Biblia, na walio kama wao, hawakulazimishwa kuingia vitani kulinda nchi wala kujilinda nafsi zao. Kwa hivyo ilikuwa ni haki wao watoe kodi kuwa ni badala ya ulinzi na manufaa mengine ya dola wanayo yapata na wanastareheha nayo. Pia ni badala ya wanacho kitoa Waislamu. Kwani Muislamu anatozwa ile khumsi (moja katika tano) ya ngawira, anatozwa Zaka ya mali, na Zaka ya Fitri, na kafara mbali mbali kwa kulipia makosa. Kwa hivyo ikawa hapana budi kuchukuliwa kodi kutokana kwa asiye kuwa Muislamu badala ya yote anayo yatoa Muislamu kwa maslaha ya wote na kwa ajili ya mafakiri wa wasio kuwa Waislamu. Wala haikukusudiwa kutozwa kodi kuwatia unyonge au kuwatia adabu. Kwani hayo hayaambatani na uadilifu wa Uislamu, wala hayakubaliani na makusudio yake mazuri.

9:30 - Uzair ndiye Ezra, Kuhani katika ukoo wa Harun. Alitoka Babilonia walipo rejea Mayahudi mara ya pili, baada ya kufa Mtume wa Mwenyezi Mungu Musa, a.s. kwa

kiasi ya miaka elfu. Na huyo Uzair akiitwa “Katibu” kwa kuwa alikuwa akiandika Sharia ya Musa.

Angalia: Uzair pamoja na Mayahudi wengine walitoka huko Babilonia kwendea Yerusalemu katika mwaka 456 K.K. (Kabla ya Kristo) katika enzi ya Arikhtisna, Mfalme wa Iran baada ya kuteketezwa Yerusalemu na kuunguzwa Baitul Muqaddas na kunajisiwa kwa muda mrefu.

9:40 - Hilo pango alilo jificha Nabii s.a.w. na rafiki yake Abu Bakar r.a. lilikuwa katika mlima wa Thor, karibu na Makka. Wakakaa humo siku tatu, baadae wakatoka usiku walipoona msako umetulia. Walifika Madina taarikh 8 katika Mwezi Rabii’ul awwal (Mfungo Sita) mwaka wa kwanza wa Hijra. (20 Septemba, 630 kwa taarikh za Kizungu.)

9:41 - Na katika maana yaliyo kusudiwa hapa ni: kuwa nendeni mmepanda au kwa miguu, mna silaha nyepesi na nyengine nzito. Na hivi ni katika mbinu maarufu za kisasa. Silaha nyepesi kama panga ni za kuuwana na askari, na silaha nzito ni za kubomoa ngome za maadui.

9:60 - Zaka ni mpango ulio wekwa wa kukusanya mali kutokana na matajiri na kurudishiwa mafakiri. Kwa hivyo ni haki ya mafakiri katika mali ya matajiri. Na huyakusanya mtawala na huyatumilia kwa njia zake ambazo zinahisabiwa kuwa ndio muhimu kabisa na bora hizo ni kupiga vita athari za ufakiri kwa mafakiri. Hupewa mafakiri, masikini, wasafiri, kusaidiwa mwenye deni aliye kopa kwa jambo la halali si kwa uharibifu, na katika hayo ipo njia ya kupewa mkopo “*kardhan hasanan*” (mkopo kwa Lillahi). Katika mwanzo wa Uislamu ilivyo kuwa Zaka inatozwa na kutumiwa vilivyo hapakuwapo katika umma mtu anaye lala na njaa, wala mwombaji aliye dhalilika kwa haja. Ilifika hadi hata wenye kutumikia Zaka wakashitaki kuwa jinsi ya kuenea neema hapana wa kustahiki kupewa. Alishitaki mmoja wapo katika Afrika kumshitakia Khalifa Umar bin Abdulaziz kuwa hakumpata fakiri wa kumpa Zaka. Umar akamwambia walipie wenye madeni. Akawalipia. Bado akashitaki tena. Akamwambia wanunue watumwa uwape uhuru wao. Huo basi ndio utumiwaji wa Zaka. Na ukitaka kweli, ni kuwa lau kuwa Zaka zikikusanywa kwa inavyo faa, na zikatumiwa zinavyo stahiki basi huo bila ya shaka ungeli kuwa ni mpango bora kabisa wa kudhamini maisha ya umma yasipate shida ya umasikini.

9:107 - Msikiti ulio tajwa katika Aya ulijengwa na baadhi ya wanaafiki wa Madina walio azimia shari. Waliudhika kujengwa Masjid Qubaa walio ujenga Banu Amri bin Auf, na akaubariki Mtume s.a.w. kwa kusali ndani yake. Basi Ibn Aamir Arrahib (aliye itwa Rahib, Mmonaki, kwa kushirikiana kwake na Mapadri) aliwachochea hao wanaafiki wajenge nao msikiti wa ushinde kushindana na walio jenga Masjid Qubaa, ili uwepo ushinde wa kijahili kwa kila mmoja kujitapa kwa kujenga msikiti. Vile vile ilikuwa azma yao wafanye hapo ni kioteo pa kukutania siri kupanga njama za kuwadhuru Waumini. Baada ya kwisha jenga walimualika Mtume s.a.w. ende kusali humo, wafanye hiyo sala ndio ada tena ya ushindani wao na kuwafarikisha Waumini. Mtume alitaka kuitikia wito wao bila ya kujua njama zao. Lakini Mwenyezi Mungu

Mtukufu alimjuvya alipo kuwa anarudi kutoka vita vya Tabuk na azma yake ya kuitikia wito. Na Yeye Subhanahu akamkataza asisimame kabisa katika msikiti huo, licha ya kusali ndani yake.

9:117 - Vita hivi vilikuwa mwezi wa Rajab mwaka wa 9 wa Hijra, baina ya Waislamu na Warumi. Na huitwa “Vita vya Dhiki”, *Ghazwatu U’sr*, kwa sababu ya dhiki ya Waislamu waliyo kuwa nayo kwa ukosefu wa mali na zana. Katika vita hivi alijitolea Othman kulizatiti jeshi zima.

10:3 - Mwenyezi Mungu ameumba viumbe vyote kwa vipindi sita, na vipindi hivi ni viwango vya mamilioni ya makarne na makarne. Na hivyo ndivyo vinavyo itwa Siku Sita. Na katika kila nguzo za ulimwengu zipo Ishara wazi zilizo zagaa za kuonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Miongoni mwa hizi, ni hivi kufanywa jua na mwezi na nyota kunyenyekea kwa faida ya binaadamu. Na kadhaalika kupishana zamu usiku na mchana, na kuwa mchana unaingilia kiza cha mbingu. Na umetajwa usiku mbele kwa kuwa kiza ndio asli. Ama mchana umezuka kwa kuathirika kwa mwangaza wa jua katika anga la ardhi, ambayo hiyo ardhi inazunguka wenyewe kwa wenyewe kama pia ili ipate mwangaza wa jua, mara upande huu na mara upande huu.

10:5 - Aya hii ya 5 inahakikisha ukweli wa kisayansi ambao haukujuulikana na hiyo sayansi ila hivi mwishoni. Hapo kwanza haukujuulikana, nao ni kuwa jua ni umbo lenye kuwaka moto, na ndio chanzo cha nguvu za kufanyia kazi zote, kwa Kiarabu huitwa *T’aaqa*, na kwa Kiingereza Energy, na kwa Kiswahili cha sasa Nishati. Katika nguvu hizo ni huo Mwangaza na Joto. Ama mwezi hauwaki moto, bali unarudisha mwangaza wa jua, kama kioo, kwa hivyo huonekana una nuru. Kwa hivyo Subhanahu ameeleza kuwa jua lina mwangaza wa asli, na mwezi unatoa nuru tu. Na Aya hii imeashiria hakika ya nyendo za falaki, nayo ni kuwa mwezi unaizunguka ardhi, na kila siku unakuwa katika mahala fulani kwa mintarafu ya dunia. Ukimaliza mzunguko wake ndio unatimia mwezi, huu wa siku 30 au 29. Kwa hivyo tunaweza kujua kiasi cha mwaka, na kwa hivyo twaweza kujua hisabu za miaka, miezi na siku.

10:6 - Aya hii ya 6 inaashiria hakika inayo onekana, nayo kukhitalifiana urefu wa usiku na mchana kwa mwaka mzima katika pahala popote duniani. Na kadhaalika kufuatana mchana na usiku, na kuwa mchana ni wa kuangaza na kuonana, na usiku ni giza. Na maana ya hayo ni kuwa msingi wake ni kuwa dunia inazunguka wenyewe kwa wenyewe kama pia juu ya msumari wake, na vile vile inalizunguka jua. Na yote hayo ni dalili ya uwezo wa Mwenyezi Mungu katika kuanzisha uumbaji. Ujuzi wa mambo hayo wakati wa Mtume s.a.w. haukuwepo. Na hii ni dalili nyengine ya kwamba haya hayakuwa ila ni wahyi, ufunuo, ulio toka kwa Mwenyezi Mungu kumpa Mtume s.a.w.

10:24 - Aya hii inaashiria ukweli ulio anza kuchomoza, nao ni kuwa mwanaadamu kwa kuifanya ilimu imtumikie ameweza kuyamiliki anayo yataka. Hata inapo kuwa karibu ya kufikilia ukweli huu kukamilika, na akaona huyo mwanaadamu amekwisha fikilia kilele cha ujuzi, hapo basi amri ya Mwenyezi Mungu hutokea.

10:92 - Inaonyesha Aya hii tukufu kuwa mwili wa Firauni utabaki umehifadhiwa ili watu wauone, na wapime kwa macho yao hali ya ule mzoga wa yule aliye kuwa akijiona ni mungu, na akiwaambia watu wake wanao mnyenyekea: Hamna mungu ila mimi!

Kadhaalika tujue kuwa kutoka Wana wa Israili katika nchi ya Misri kulikuwa mwishoni mwa karne ya kumi na tatu kabla ya kuzaliwa Nabii Isa a.s., katika enzi ya mmoja wa Mafirauni wa Ukoo wa kumi na tisa, naye ni Minfitah mwana wa Ramsis wa Pili, ambaye ndiye aliye wakandamiza Wana wa Israili akawalazimisha wamjengee Jiji la ufalme wake.

Uvumbuzi wa machimbo ya vitu vya kale wa hivi karibuni umedhihirisha kuwa jina la mji huo ulio funikika chini ya ardhi, ni “Bur’amsis”. Kulikuwa kutoka kwa Wana wa Israili pamoja na Musa ni kwa ajili ya wito wa Tawhidi, Umoja wa Mwenyezi Mungu, na kuikata shemere ya Firauni iliyo wadhhalilisha, na ikawakutisha adhabu ya mwisho. Na ilikuwa haijuulikani na Waarabu ambao hawajui kusoma na kuandika, wala kwa wengineo, kwamba mwili wa Firauni huyu ungalipo mpaka hii leo. Lakini Qur’ani imeyataja hayo, na ukweli wake umethibiti mwaka 1900 B.K., yaani karne kumi na tatu baada ya kuteremka Qur’ani. Je, hii si dalili ya kuwa imetoka kwa Mungu?

10:101 - Aya hii na Aya nyingi nyenginezo zinaita watu wajifunze kwa kuangalia na kuzingatia (Observation). Na inaita watu wajifunze ilimu ya ulimwengu na viliomo ndani yake, kwani huo ulimwengu umedhalilishwa kwa ajili ya mwanaadamu. Kisha hizo Aya zinataka watu waingie katika ilimu za kujaribu (Experimental Science). Kwani hiyo ni njia ya kujua kwa kuona vinavyo onekana.

11:13 - Qur’ani si muujiza tu katika maandishi yake, bali ndani yake mna hadithi za kweli, na ilimu mbali mbali za sayansi za uumbaji zilizo ashiriwa, na hazikuwa zikijuulikana wakati wa kuteremka kwake, na pia katika hukumu ziliomo ndani yake. Hao ambao hima yao ni kushughulikia dunia tu, Akhera hawana lao jambo ila adhabu ya Motoni, na kuharibikiwa na yote waliyo yafanya duniani, kwa sababu hawakuwa na fungu lolote katika Akhera. Na hayo wayatendayo pia yatakuwa yameharibika vile vile, kwani kitendo kisicho leta mafanikio ya daima ni kama kwamba hakikupata kuweko.

11:17 - Mwenyezi Mungu amemuamrisha Nabii s.a.w. asitie shaka, si kwa kuwa yawezekana kuwa yeye awe na shaka, lakini ni kuashiria kuwa walio kuwa duni yake Nabii wajilinde wasiache shaka ikaingia nyoyoni mwao.

11:44 - Mlima huo uko Mosal (kaskazini mwa Iraq na kusini ya Turki) Ulikuwa maarufu hapo kale.

11:84 - Hizi Aya mbili zinakataza kupunja kwa vipimo na mizani kwa kuwa ni ukhalifu unao stahiki kupewa adhabu na kuaziriwa. Makosa haya ya kupunja na udanganyifu pia yanahisabiwa ni ukhalifu hata katika kanuni za kutungwa za dikrii. Na katika Qur’ani tukufu ni moja katika njia ya kulinda mali. Nchi ya Madyana ipo baina ya kaskazi ya Hijazi na kusini ya Sham. Na hii ilikuwa imejaa miti. Ikiitwa *Al-*

aykah,(yaani Machakani). Na Mwenyezi Mungu aliwapelekea adhabu kwa sababu ya uasi wao.

12:4 - Yusuf, *Alayhi Ssalam*, alikuwa mwana wa Yaaqub, Muabrani, Mkanaani. Akauzwa Misri katika enzi ya utawala wa wavamizi wa kigeni waitwao Wahiksos. Na kwa ionekanavyo hao Wahiksos ni katika kabila za Kisami walio ingia Misri kutoka Sham wakaiteka Delta ya Misri mnamo mwaka 1730 k.k. (kabla ya Nabii Isa a.s.) na kabla ya kumalizika enzi ya ukoo wa kumi na tatu wa Mafirauni. Wakaihukumu Misri kwa muda wa karne unusu. Wakafukuzwa mnamo mwaka 1580 k.k. na Ahmas wa Mwanzo aliye anzisha ukoo wa 18. Wakatolewa nje ya mipaka ya Misri.

12:47 - Aya hii inawafikiana na ilimu za kisasa kuwa kuweka punje katika mashuke yake inakuwa ni hifadhi zisiharibike kwa hali ya hewa na mengineyo, na juu ya hivyo faida yake ya chakula inabaki kwa ukamilifu zaidi.

12:84 - Huzuni kubwa huleta ugonjwa wa macho unao itwa Glocoma, na weupe huzidi mpaka mtu mwisho anakuwa kipofu.

13:3 - Mwenyezi Mungu Mtukufu amejaalia katika kila mimea dume na jike ili ipate kupandishika sehemu ya uke kwa chembe za uzazi zilioko katika sehemu za ume. Na kwa hivyo ndio huzalikana namna kwa namna na kwa wingi.

13:4 - Aya hii tukufu inaonyesha ilimu ya ardhi (Geology) na ilimu ya mazingira (Ecology) na athari yao juu ya sifa za mimea. Inajuulikana katika ilimu kuwa rutuba ya ardhi inategemea juu ya chembe chembe za maadeni zinazo khitalifiana kwa namna na ukubwa, na maji yanayo toka kwenye mvua, na hewa, na vitu vyenye asili ya uhai, kama mimea na vyenginevyo, ambavyo hupatikana juu ya udongo au ndani yake. Huwapo hivyo kwa mamilioni vidogo vidogo hata havionekani kwa jicho tu. Kwa jumla ukizingatia haya utaona yanaonyesha uwezo wa Muumba na busara ya umbaji, kwani ardhi kama wasemavyo wakulimu inakhitalifiana kila shubiri.

Na inajuulikana kwa wanazuoni wa sayansi kuwa ukipatikana upungufu katika hivyo vitu vya msingi katika udongo basi hudhihirisha upungufu wake katika mimea, na kwa hivyo wakulima hujalizia upungufu huo kwa kutia mbolea mbali mbali na hutengeneza hali ya mazingira. Na hayo yana athari zake juu ya mazao ikiwa kwa mmea wa namna moja au namna mbali. Ametakasika Mwenyezi Mungu ambaye katika mikono yake upo ufalme wa kila kitu, naye ni Muweza wa kila kitu.

13:41 - Aya hii ina ukweli ulio fikiliwa na uchunguzi wa kisayansi za hivi sasa, ya kwamba imethibiti kuwa dunia inazunguka, na kuwa inayo mvuto kama simaku. Hayo yamepelekea kubabataa katika ncha mbili za kaskazini na kusini, North Pole na South Pole. Na hivyo ni kupunguka katika ncha mbili za ardhi. Na kadhaalika imejulikana kuchopoka mbio za sehemu za gasi zilizo funika huu mpira wa dunia kukipindukia nguvu za mvuto wa ardhi, basi hutoka nje ya dunia. Na haya yanatokea mfululizo, na kwa hivyo ardhi, yaani dunia, inakuwa katika hali ya kupunguka moja kwa moja katika ncha zake. Haya yanakuwa kwa kuifasiri ardhi kuwa ni dunia, si nchi

ya maadui wa Waumini. Yaelekea tafsiri hii kwa Aya hii tukufu, ijapo kuwa wafasiri wengi wamefasiri kuwa muradi wa “ardhi” ni nchi za maadui.

15:19 - Aya hii inaeleza uhakika wa uumbaji ambao haukujuulikana ila katika zama za hivi karibuni. Nayo ni kuwa kila kabila ya mimea imefanana kati yao kwa kuonekana na undani wake, hata katika sehemu zake ndogo ndogo, katika viungo vyake vyote vya hiyo mimea. Na hali kadhaalika katika “Khalaya” au “Cells” za hiyo mimea ya kabila fulani, kwa ajili ya kutimiza kazi iliyo kusudiwa kiungo hicho cha mmea. Na pia sehemu za mimea ya hizo kabila zao na vilivyo undwa katika viungo vyake utaona mnasaba wake umethibiti kila mwaka, ukilinganisha kwa wakati ule ule katika miaka mingine.

15:22 - Aya hii imeitangulia sayansi kwa kusema kuwa upepo unafanya kazi kubwa katika kubeba pollen, chembe dume za kupandishia mimea, kupelekea sehemu za uke za mimea mingine, na kwa hivyo yakazalikana mazao. Na pia haikujuulikana ila mwanzo wa karne hii tuliyo nayo (ya ishirini) kwamba upepo unazalisha mawingu yanayo nyesha mvua. Kwani “Nucleons” ambazo juu yake hujumuika sehemu za mvuke wa maji na zikawa chembe chembe za maji ndani ya wingu, ndizo chanzo cha mvua inayo chukuliwa na pepo kupelekwa kwenye majimbo yanayo fikiwa na mawingu. Misingi ya hizo “Nucleons” ni chumvi ya bahari, na vinavyo chukuliwa na upepo juu ya uso wa ardhi, na “Oxides” na vumbi vumbi, n.k. Na vyote hivyo ni lazima kwa ajili ya mvua.

“Wala si nyinyi mnayo yaweka”. Imethibiti kwa sayansi ya kisasa kuwa mvua inaanza kwa mvuke kutokana na uso wa ardhi na bahari, kisha inarejea hali ile ile tena kama ilivyo tajwa. Ikinya mvua hunywesha kila kilicho na uhai katika ardhi, na huinywesha ardhi yenyewe. Wala haiwezekani kuzuilika, kwa sababu ikichuruzika kutokana na vyote vyenye uhai na katika ardhi ikaingia baharini, tena kisha huanza kuzunguka mara ya pili kwa kupanda mvuke kutoka baharini. Basi hali ni hivyo mzunguko. Hapa ndio inabainika maana ya Aya “Wala si nyinyi mnayo yaweka.”

15:53 - Inaonyesha hapa kuwa bishara hii si ya Ismail a.s. Kwani Ismail alikuwa kesho zaliwa, naye na mama yake Haajir walikuwa wapo Makka. Bishara hii ni ya Ibrahim na mkewe, basi kwa hivyo ni ya Is-haq mwana wa Ibrahim na Sara.

15:80 - Watu wa Hijr ndio Thamud. Na Hijr ni bonde baina ya Madina na Sham. Tazama maelezo juu ya Aya 73 ya Surat Al-Aa’raaf.

16:49 - Aya hii imeitangulia sayansi kwa kusema kuwa katika baadhi ya sayari upo uhai katika mfumo huu wetu wa jua, au nje yake. Sayansi sasa inajaribu kutaka kuvumbua hayo.

16:65 - Maji huteremka kutoka mbinguni kuangukia ardhini, na huko huyayusha chumvi chumvi zake za namna mbali mbali ambazo hunyonywa na mimea kugeuka kwenye uhai.

16:66 - Katika viwele vya wanyama wa mifugo imo namna ya mitoki (glands) ambayo inachuja maziwa. Mitoki hiyo inanyweshwa na mishipa inayo leta madda maalumu kutokana na damu, na (chyle); hicho ni chakula kilicho tayarishwa. Viwili hivyo huwa vimekwisha lainishwa kwa kumezwa kama ni chakula. Kisha hapo hizo glands za maziwa huteuwa sehemu yenye kuhitajiwa kwa kufanya maziwa kutokana na vitu viwili hivyo, damu na chyle, na humiminiwa maji maalumu kugeuza hivyo vikawa maziwa yenye kukhitalifiana na asili yake kwa rangi na utamu kabisa.

16:69 - Asali ya nyuki ni mchanganyiko wa glucose na livulose, nayo ni namna ya sukari ambayo ni nyepesi kabisa kutumika mwilini, na madaktari wamevumbua karibu kuwa glucose ina faida kutibu maradhi mengi, kwa kupiga sindano, na kwa mdomo na kwa nyuma, kwa kuwa inatia nguvu, na inapinga sumu ya maadeni kadhaa wa kadhaa, na sumu inayo patikana kwa maradhi ya viungo, kama kuingia sumu kwa mkojo na maradhi ya kuwa manjano (jaundice) na mengineyo. Vile vile imethibiti kuwa Vitamin nyingi hupatikana humo, na khasa Vitamin B complex.

16:72 - Ndoa ni mfungamano mtakatifu ambao ndio asili ya ukoo na kiini cha umma na jamii. Na ndoa ni mpango wa kuidhibiti ile khulka waliyo nayo wanaadamu na wanyama, nayo ni kutamani kuingiliana. Lau ingeli kuwa hapana ndoa iliyo kadiriwa kudhibiti ile khulka ya kutamaniana basi binaadamu wangeli kuwa sawa na wanyama kwa kufuata fujo na uchafu wa kuingiliana. Na hapo mwanaadamu asingeli kuwa yule kiumbe aliye mjaalia Mwenyezi Mungu kuwa na akili na fikra na akamtukuza kuliko viumbe vyengine, na akamrithisha mamlaka ya ardhi. Iliyoy kuwa mpango wa Mwenyezi Mungu katika uhai huu ni kutengeneza khulka kwa ndoa ili binaadamu awe juu kuliko wanyama wengine, hali kadhaalika binaadamu kwa upande mwengine ameumbiwa kupenda kubakia. Na ilivyo kuwa hapana njia ya kubakia yeye mwenyewe, naye anayajua hayo kutokana na baba zake na babu zake na vitu vyote vilio hai, basi njia pekee ni yeye kuzaa dhuriya wapate kuishi na kuendelea daima. Na labda lenye kuweka wazi kabisa ile khulka yake ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni wake katika jinsi yenu, na akakujaalieni kutoka kwa wake zenu wana na wajukuu, na akakuruzukuni vitu vizuri.”

16:78 - Utabibu wa kisasa umethibitisha kuwa kuweza kusikia kunaanza mapema sana katika maisha ya mtoto mchanga, mnamo wiki chache za mwanzo. Ama kuona huanza mwezi wa tatu. Wala kuona hakuwi baraabara mpaka katika mwezi wa sita. Ama “moyo “ wa kufahamu na kutambua huwa baada ya hayo. Mpango ulio letwa na Qur’ani ni mpango unao lingana na hisiya hizo.

16:79 - Ndege wanaruka kwa sababu kadhaa wa kadhaa katika kuumbwa kwao. Muhimu kuliko yote ni lile umbo lao la kuchongoka, na kuwa mbawa zao zilivyo tanda zenye manyoya, na mafupa yenye uwazi na myepesi na vifuko vya hewa kati ya matumbo yao, navyo vimeambatishwa na mayavuyavu (mapafu). Hivyo vifuko hujaa hewa wakati wa kuruka, basi huzidi hao ndege kuwa wepesi.

16:92 - Aya mbili hizi zinaonyesha kuwa msingi wa makhusiano baina ya Waislamu na wengineo pamoja na uadilifu ni kutimiza ahadi, na kwamba makhusiano baina ya mataifa hayasimami sawa ila kwa kutimiza ahadi, na kwamba dola za Kiislamu zikijifunga kwa mapatano basi zijifunge kwa jina la Mwenyezi Mungu. Maana ya hayo ni kuwa inakuwapo yamini ya Mwenyezi Mungu na kuwa Yeye ndiye dhamini. Na Aya inafahamisha mambo matatu, ambayo lau kuwa mataifa yangeli yatimiza basi amani ingeli enea:

* Kwanza: Haifai mapatano kuwa ndio njia ya kufanya khadaa. Ikiwa hivyo inakuwa ni udanganyifu. Na udanganyifu haufai katika makhusiano baina ya wanaadamu, sawa sawa ikiwa baina ya mtu na mtu, au kikundi na kikundi, au baina ya madola.

* Pili: Kutimiza ahadi peke yake ni nguvu. Na mwenye kuvunja ahadi ni kama mwenye kuvunja alichokijenga kwa sababu za nguvu. Basi anakuwa kama mpumbavu anaye tatua uzi wake kila akisha usokota.

* Tatu: Haimfalii mtu kuvunja ahadi kwa sababu ya kutafuta nguvu au kutaka kuzidisha kipande cha ardhi.

17:101 - Hizo ishara tisa ni: 1. Fimbo, 2. Mkono Mweupe, 3. Tufani, 4. Nzige na vyura na chawa na damu, 5. Ukame na upungufu wa mazao, 6. Kupasuka bahari, 7. Kutimbuka maji baharini, 8. Kuning'inia mlima kama kivuli, 9. Kusemezwa na Mola wake Mlezi.

18:16 - Haijuulikani kwa hakika ni nani hao Ahlil Kahf, wala zama zao, wala hilo pango lipo wapi walilo kimbilia hao vijana. Pamoja na hayo hapana ubaya kuchunguza, huenda pakapatikana mwangaza japo kidogo juu yake. Iivyo kuwa Qur'ani Tukufu imetaja kuwa hao walikuwa ni vijana walio muamini Mola wao Mlezi basi hapana budi kuwa wao na watu wao waliteswa kwa sababu ya Dini, hata wakaona hao vijana wakimbilie pangoni kujificha. Na Taarikhi ya zamani inataja kuwa yalikuwako mateso ya dini katika nchi za Mashariki ya kale yaliyo tokea nyakati mbali mbali. Tutataja katika yafuatayo mateso mawili huenda moja wapo likaelekea na kisa hichi:-

Ya kwanza yalitokea zama za mfalme wa Kisaluki, Antiokhus IV, aliye itwa kwa jina la kupanga Nabivanis (kiasi ya 176-84 K.K.). Huyo alipo shika ufalme wa Shamu, na akawa amemili mno kwenye ustaarabu wa Kigiriki na ilimu zake, aliwalazimisha Mayahudi wa Palistina, nayo ilikuwa chini ya Shamu tangu mwaka 194 K.K. washike dini ya Kigiriki, na akavunja sharia zao, na akanajisi Hekalu lao kwa kuweka humo sanamu la Zeus, mungu mkuu wa Magiriki, juu ya madhibahu (kibulani), na kumtolea mihanga ya nguruwe humo. Tena huyo mfalme alitekteza kwa moto nakla za Taurati zote alizo zipata. Kwa mwangaza huu yaonekana kuwa hawa vijana walikuwa ni Mayahudi, na kwao ni popote katika Palastina, au khasa ni katika Yerusalemu. Na ikawa wakaamka mnamo mwaka 126 B.K. zama za utawala wa Warumi wa Mashariki. Yaani kabla ya kuzaliwa Mtume Muhammad s.a.w. (nako kulikuwa kiasi mwaka 571 B.K.) kwa kiasi ya miaka mia nne na arubaini na tano takriban.

Ama mateso ya pili yalitokea zama za Mfalme wa Ufalme wa Kirumi, Hadriatus (117-138). Mfalme huyu aliwatenda Mayahudi kama alivyo watendea Antiokhus tuliye kwisha mtaja sawa sawa. Matokeo ya hayo ni kuwa Mayahudi walitangaza uasi dhidi ya utawala wa Kirumi mwaka 132. Wakawafukuza askari wa ulinzi wa Kirumi,

wakaiteka Yerusalemu, na wakatoa sarafu yao ya makumbusho ya ugombozi wa Mji Mtakatifu. Wakashika khatamu za utawala kwa muda wa miaka mitatu. Mwishoni Hadriatus na jeshi lake wakagutuka, wakaushinda uasi, na wakairudisha Palastina chini ya ut'iifu, na wakairudisha Yerusalemu, na wakauvunjilia mbali uwananchi wa Kiyahudi kabisa. Viongozi wa Mayahudi wakauwawa na Mayahudi wakauzwa sokoni kuwa watumwa. Matokeo ya hayo ni kuwa mambo yote ya Kiyahudi aliyapiga marfuku Hadriatus na akapiga marfuku mafunzo ya Kiyahudi na sharia zao.

Kwa mujibu wa mwangaza huu wa taarikhii yaonekana kuwa vijana hawa walikuwa ni Mayahudi, na pahala pao ni popote katika Mashariki ya kale, au katika Yerusalemu yenyewe. Yaonekana kuwa waliamshwa mnamo mwaka 435 B.K., yaani kabla ya kuzaliwa Mtume wetu s.a.w. kwa miaka mia na thalathini. Yaonekana kuwa yale mateso ya mwanzo yameelekeana zaidi na kisa hichi cha Watu wa Pangoni, kwa sababu yalikuwa ni ya shida zaidi. Ama mateso ya Kikristo hayaelekeani na kuzaliwa kwa Mtume s.a.w.

18:25 - Aya hii inaonyesha ukweli wa ilimu ya Falaki (Astronomy), nayo ni kuwa ni miaka 300 kwa mwendo wa jua, na miaka 309 kwa hisabu ya mwezi unao fuatwa na Waislamu. Aya hii imeitangulia ilimu ya Falaki.

18:93 - Hiyo ngome au boma baina ya milima miwili iliyo tajwa katika maelezo ya juu ni milima ya Azarbajan na Arminia, na kauli nyingine ni kaskazini ya mwisho katika jimbo la Turkistan.

18:101 - “Wale ambao kwamba macho yao yalikuwa paziani hayanikumbuki, na wakawa hawawezi kusikia”: Ni wale ambao macho yao yameghafilika na kunizingatia Mimi katika mbingu na ardhi. Na kwa hivyo hii Aya tukufu inazindua watu wazingatie yote yalio wazunguka yanayo onyesha Ishara za kuwepo Mwenyezi Mungu.

19:25 - “Na litikise kwako hilo shina la mtende, utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu.” Imethibiti kuwa tende, khasa zile rat’ab, yaani “fresh” zina faida kubwa sana katika mwili, na nyepesi katika tumbo.

19:28 - “Ewe dada wa Harun! Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba.” Imeandikwa katika Encyclopaedia Britannica kuwa Qur’ani imekosea kosa la kihistoria ilipo mwita Maryamu “Dada wa Harun,” ilihali baina ya Maryamu huyu na Harun nduguye Musa ni karne nyingi. Wamesahau hawa kuwa Udugu kwa Kiarabu upo kwa kushabihiana. Makusudio ya hapa ni kushabihiana kwa wema na kuchamngu, yaani ewe uliye mshabihi Harun kwa wema na uchamngu, nini kilicho kugeuza hali yako njema ukawa hivyo? Wala baba yako hakuwa mtu muovu wa kutenda mabaya, wala mama yako kufanya uchafu. (Kadhaalika Maryamu ni ukoo wa Harun, na pengine huitwa “Binti wa Imran”, na Imran ni baba yake Harun.)

20:50 - “Akasema: Mola wetu Mlezi ni yule aliye kipa kila kitu umbo lake, kisha akakiongoa.” Mwenyezi Mungu Subhanahu amekijaalia kila kiumbe kina sifa zake makhsusi za kutekeleza kazi yake kilicho umbiwa nacho katika maisha, kama alivyo

pewa hidaya mwanaadamu.

21:30 - “Je! Hao walio kufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi tukazibabandua? Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini?” Aya hii ina maana ya kisayansi yenye kutilia nguvu nadhariya ya ilimu za kisasa katika kuumbwa sayari na ardhi. Nayo ni kuwa mbingu na ardhi asili yao zilikuwa zimeshikamana. Na ukweli wa sayansi zinazo kubaliwa ni kuwa hakika ziliambatana, na sayansi mbali mbali zinathibitisha hayo. Na zipo nadhariya nyengine kadhaa wa kadhaa ambazo kwazo zaweza kuelezea dhaahiri ya mambo haya. Lakini bado kuthibiti nadhariya mojawo kwa njia ya mkato kwa wanazuoni kwa kuwafikiana wote. Kwa kuonyesha mfano tutaja nadhariya mbili:

Nadhariya ya Kwanza: Imekhusu kuumbwa kwa mfumo wa jua (Solar System). Kwa mfano imethibiti kuwa mawingu au umande ulio zunguka jua ulianza kuenea kwenye anga lililo baridi, na chembechembe za gasi zinazo fanya hayo mawingu au moshi zikakusanyika kwenye chembechembe za vumbi linalo kwenda kwa kasi kubwa. Kisha chembechembe hizo zikawa zinagongana na zinarindika, na huku ndani yake zikawamo gasi nzito, na kukazidi kurindika na kujumuika kwa kupita mamilioni na mamilioni ya makarne mpaka zikafanyika sayari na mwezi na ardhi kwa umbali unao stahiki. Na yajuulikana kuwa huko kukusanyika na kurindika huzidisha mbinyo (Pressure), na huo huzidisha joto. Na gamba la ardhi lilipo ingia kupoa, na wakati zilipo ripuka volkano ardhi ikapata mvuke wa maji na gasi ya Carbon dioxide ilio tokana na miripuko ya volkano na katika iliyo saidia kupatikana Oxygen katika hewa baada ya hapo ni nishati na nguvu za miyale ya jua kwa njia ya mwanga juu ya mimea na majani ya mwanzo.

Ama Nadhariya ya Pili: Imekhusiana na uumbaji wa ulimwengu kwa jumla, ambao kwa mukhtasari unaelezwa na kauli yake Mtukufu: “Zilikuwa zimeambatana”, yaani zimeshikamana na kuwa kitu kimoja. Na hayo ndiyo yaliyo fikilia mwishoni ilimu za sayansi katika uumbaji wa ulimwengu. Nayo ni kwamba kabla ya kufikilia sura yake hii ya sasa ulikuwa kama donge lililo kusanyika lenye kutisha, la mkusanyiko wa chembechembe zenye kuambatana chini ya mbinyo pressure, hata akili haiwezi kuifikiria. Na hizi sayari zote na nyota zilioko mbinguni hivi leo tunazo ziita mfumo wa jua solar system zilikuwa ni mkusanyiko wa donge moja lisilo zidi 1/2 diameter yake maili milioni tatu. Na neno lake Mwenyezi Mungu: “Tukazibabandua” linafahamisha ule mripuko mkubwa wa mwanzo wa ki-nuclear ukazalisha uumbaji wa anga na sayari za namna mbali mbali tunazo ziita kwa pamoja “Mfumo wa Jua” au Solar System.

“Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai”: Aya hii imethibitisha uhakika wa kisayansi ulio thibitishwa na ncha mbali mbali za ilimu. Imethibitisha Cytology, sayansi ya “cells”, (khalaya), kwamba maji ni muhimu kabisa katika ujengaji wa “cells” zote za vitu vilivyo hai, ikiwa mimea au wanyama. Na ilimu ya “Kimyaa”, Chemistry kwamba maji ni lazima yapatikane katika vitendo na mageuko yoyote katika viumbe vilivyo hai. Basi hayo maji ama yawe ni kiungo, kitu cha kusaidia, au cha kuwamo ndani ya kitendo, au ni matokeo yake.

Na imethibitisha ilimu ya viungo physiology kwamba maji ni dharura kwa viungo kufanya kazi yao. Bila ya hayo maji hautodhihiri uhai katika viungo.

21:31 - Maoni ya wataalamu juu ya Aya ya 31:

“Na tukaweka katika ardhi milima iliyo thibiti ili isiwayumbishe, na tukaweka humo njia pana ili wapate kuongoka.” Ilivyo kuwa ndani ya ardhi kila kitu kimeyayuka, na lau kuwa milima imewekwa tu katika baadhi ya sehemu za huu mpira wa dunia kama majabali yaliyo nyanyuka juu tu, uzito wao ungesi sabibisha gamba la dunia liyumbe, au lipindane na kupasuka. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu kwa utukufu wa shani yake ameifanya milima isimame imara kwa kuwa na mizizi iliyo zama kwenye gamba la ardhi mpaka chini kwenye kina kirefu kulingana na urefu wake kwendea juu. Kwa hivyo imekuwa hiyo milima kama vigingi, kama alivyo jaalia eneo la minyanyuka hii na mizizi ni duni kuliko maeneo ya gamba lilio zunguka. Yote haya ni kwa ajili ya kueneza sawa uzito wa juu ya gamba kwa pande zote ili pasiwepo kuyumbayumba na kupasuka. Kwani hakika kuenezwa kwa uzito juu ya uso wa dunia yakaribia kuwa hakuleti athari kubwa ya kutajika.

Na ilimu za kisasa zimethibitisha kuwa kuenezwa kwa nchi kavu na maji juu ya ardhi, na kuwepo mfululizo wa milima juu yake ni katika yanayo hakikisha hali ilivyo ardhi, na imethibitika kuwa chini ya milima mizito kuna vitu vyepesi kubungunyika, na chini ya maji ya bahari kuu vipo vitu vizito. Kwa kuenezwa uzani wa namna hiyo mbali mbali katika dunia, na mgawanyo huu wa milima, makusudio yake ni kusawizisha uzani wa mpira huu wa ardhi. Na ilivyo nyanyuka milima zikatokea nyanda na mabonde na njia baina ya milima na mwambao na bahari na minyanyuko, na zikawa njia.

21:32 - Maoni ya wataalamu juu ya Aya 32:

“Na tukaifanya mbingu kuwa dari iliyo hifadhiwa lakini wanazipuza Ishara zake. “: Aya hii tukufu imethibitisha kuwa mbingu na vyote viliomo ndani yake vimehifadhiwa visiwe na ila yoyote, na vimehifadhiwa visidondoke juu ya ardhi. Na mbingu ni kila kilicho juu yetu, kuanzia kifuniko hichi cha hewa inayo walinda walioko juu ya ardhi na khatari nyingi za angani ambazo zinazuia maisha, mfano wa vimondo vya nyota za mkia, na miyale. Na juu ya ardhi pana kifuniko cha hewa kinacho linda ardhi kwa nguvu za mvutano, na haifai kukosekana hivyo bila ya maangamizo kabisa. Na juu ya kifuniko cha hewa ndio kuna hizo sayari za mbinguni, na zipo kwa umbali mbali mbali kufuatana na nyendo zao tangu mwanzo.

“Na tukaifanya mbingu kuwa dari iliyo hifadhiwa” yaani hizo sayari na vyote vilio mbinguni vyaonekana kwa nadhari yetu kama kwamba ni dari, na tunaona vilio juu ya vichwa vyetu kama ni vidogo kuliko vilioko upeo wa macho. Na hayo ni kiini macho tu, kama tunapo liona jua kubwa wakati wa kuchomoza na kuchwa kuliko aduhuri. Na hili qubba la mbingu lina sifa zake, zinazo khitalifiana kila ukizidi mnyanyuko wa ardhi, kama hizo sayari za mbinguni kwa mujibu wa jicho linavyo ona katika qubba la mbingu.

21:33 - Maoni ya wataalamu juu ya Aya 33:

“Na Yeye ndiye aliye umba usiku na mchana na jua na mwezi, vyote katika anga vinaogelea.” Kila sayari ya mbinguni ina mzunguko wake makhsusi inayo ogelea

kuufuata. Na zote hizo hazisiti, na zinakwenda kwa mwendo wao maalumu katika anga. Na sisi tunaona hayo kwa hakika kwa kutazama mwendo wa jua na mwezi. Kama kadhaalika mzunguko wa ardhi wake wenyewe ndio unao leta usiku na mchana kwa zamu, kama kwamba unaogelea.

21:37 - Maoni ya wataalamu juu ya Aya 37:

“Mwanaadamu ameumbwa na haraka. Nitakuonyesheni Ishara zangu. Basi msinihimize.” Makusudio ya kauli ya “Ishara” ni ishara za maumbile zenye kuonyesha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na uweza wake. Na ujuzi wa ilimu za sayansi utavumbua kwa mujibu wa itavyo nyanyuka akili ya binaadamu. Na hayo ni kwa mujibu wa miadi ilio wekwa kwa wakati wake. Kila ukifika wakati maalumu Mwenyezi Mungu hudhihirisha Ishara yake, au huwasahilishia wanaadamu njia za kuzifikilia Ishara hizo.

21:44 - Maoni ya wataalamu juu ya Aya 44:

“Je, hawaoni ya kwamba Sisi tunaifikia ardhi tukiipunguza mipaka yake? Basi je! Hao ni wenye kushinda?”: Aya hii ni katika Aya za miujiza ya kisayansi katika Qur’ani Tukufu. Hii inaonyesha kuwa dunia si mduwara kaamili. Na wataalamu wa sayansi hawakutamakani kupima masafa ya dunia baraabara mpaka kiasi ya miaka 250 tu takriban, walipo ingia kikundi cha mabingwa walio khusika na ilimu ya kupima marefu baina ya daraja mbili za urefu longitudes. Na hayo kwa pahala mbali mbali duniani. Katika kupima huku ikadhihiri kuwa nusu ya kati ya dunia kwenye equator inazidi kuliko nusu ya poles kwa takriban kilomita 21.5. Yaani dunia imepungua katika ncha zake, yaani katika poles. Na inajuulikana maalumu kuwa sura ya dunia na masafa yake ndio msingi katika kuchorwa kwa ramani.

21:47 - Maoni ya wataalamu juu ya Aya ya 47:

“Nasi tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali tutaiteta. Nasi tunatosha kuwa washika hisabu.”: Aya hii tukufu inaonyesha kuwa chembe ya khardali ni hadi ya udogo katika mizani. Imethibitika kwa majaribio ya sayansi kuwa Kilogram ya chembe za khardali ni chembe 913,000. Kwa hivyo chembe moja ya khardali ni takriban sehemu moja katika elfu ya gram, yaani ni takriban sawa na Miligram moja. Na huu ni uzito mdogo kabisa unao juulikana katika mbegu za mimea mpaka sasa. Kwa hivyo hutumiwa katika kupimiwa vitu vidogo vidogo kabisa.

21:78 - Kisa cha hiyo hukumu: Mbuzi waliingia usiku mmoja katika konde ya mtu, wasibakishe kitu. Daud akahukumu kuwa wale mbuzi wawe wa mwenye konde kulipia khasara yake. Suleiman akatoa hukumu nyengine, akasema: Mbuzi wale wabakie mkononi mwa mwenye konde mpaka itapo mea tena mazao yake, na avumilie kwa yaliyo mpata. Na baada yake warejesheane.

22:5 - Maurice Bucaille, mtaalamu wa Kifaransa maarufu aliye silimu, amelifasiri neno *A’laqa* kwa maana ya “kitu kilicho tundikwa”. Na hivyo ndivyo inavyo thibitisha Sayansi ya hivi sasa, kuwa mbegu ya uzazi ikisha pandikizwa huja ikaning’inia kama iliyo tundikwa kwenye tumbo la uzazi. Tazama pia 23:14, 40:67, 75:37-38 na

kadhaalika Sura ya 5 ya Annisaa Aya 129, inayo eleza kuwa msimwache mke “kama aliye tundikwa”.

22:39 - “Wameruhusiwa kupigana wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia” Yaliyo tajwa na Qur’ani Tukufu kukhusu hukumu iliomo katika Aya 39 yamezitangulia kanuni zilizo kuja kuwekwa na madola baada yake, nayo ni kuwa mtu kujitetea nafsi yake ni sharia vyovyote vile itavyo kuwa matokeo yake. Na kwamba mwenye kuitetea nafsi yake, na mali yake, na nchi yake, hawi ni mkosa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya uadilifu, ijapo kuwa ameuwa mtu au ameteketeza roho nyingi. Aya hii imepasisha kuwa Waislamu wanayo ruhusa kujitetea pindi wakivamiwa. Na kwa hivyo tunafahamu kuwa vita vya Waislamu vilikuwa vita vya utetezi na kujilinda si vita vya kushambulia na kuvamia. Na kwamba Waislamu waliusimamisha Uislamu na wakaupa nguvu kwa hoja zilizo wazi, na dalili zilizo dhaahiri.

22:47 - “Na wanakuhimiza ulete adhabu, lakini Mwenyezi Mungu hatakwenda kinyume na ahadi yake kabisa. Na hakika siku moja kwa Mola wako Mlezi ni kama miaka elfu mnavyo hisabu nyinyi.” Qur’ani kwa Aya hii tukufu imeutangulia msafara wa wana sayansi kwa kueleza kuwa zama ni kipimo cha mnasaba, na kwamba fikra ya kuwa zama kwa ulimwengu ni moja kama watu wa zamani walivyo kuwa wakifikiri ni makosa.

22:65 - “Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu amevidhalilisha kwenu viliomo katika ardhi, na marikebu zipitazo baharini kwa amri yake, na amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa idhini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye huruma kwa watu, Mwenye kurehemu.” Aya hii tukufu inakusanya maana za kisayansi za ndani. Mbingu, nayo ni kila kilicho juu yetu, inaanza kwa kuifunika ardhi kwa hewa, tena kwa anga, tena kwa vyombo vya mbinguni vinavyo toa mwanga kama nyota n.k. na visio toa mwanga wake mwenyewe kama mwezi, na sayari nyengine, na nyota mkia, na vumbi la ulimwengu, n.k. Vyote hivi vinakuwa vilivyo na vinashikana kwa athari ya nguvu mbali mbali. Muhimu wa hizo ni mvuto na nguvu inayo tokana na kule kuzunguka kwao.

Yamedhihiri mapenzi ya Mwenyezi Mungu na huruma zake kwa waja wake kuwa katengeneza kifuniko cha angani kina namna za gasi mbali mbali ambazo ni dharura kwa uhai. Kama pia anawalinda wakaazi wa duniani na mianga na vimondo n.k. vinavyo zunguka angani na ambavyo vinapo karibia kwenye ardhi huungua kabla havijafika chini.

Na katika mapenzi yake na rehema yake Mwenyezi Mungu ni kuwa hivyo vimondo vinavyo anguka kwenye ardhi ni nadra sana kutokea, na hutokea mwahala wasipo kaa watu. Jambo hili la dhaahiri laonyesha huruma na rehema ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake. Na haya yanatilia nguvu na kusadikisha kauli yake Mwenyezi Mungu: “na amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa idhini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye huruma kwa watu, Mwenye kurehemu.”

23:4 - “Na ambao wanatoa Zaka,”: Huu waajibu wa kutoa Zaka unapelekea kujenga

mashikamano ya umoja baina ya Waislamu, na kutia katika moyo wa kila mtu kuwa ana jukumu kwa nduguye, anahisi kama anavyo hisi yeye, na anaungulika kama anavyo ungulika yeye. Kwa hivyo ni waajibu wake kufanya awezavyo kumkinga na balaa za kilimwengu, na machungu ya ukosefu. Kwa hivyo fakiri au masikini hatomchukia tajiri, bali wote watahisi kama ni ukoo mmoja unao saidiana na wenye kushikamana na Kamba ya Mwenyezi Mungu. Wala mwenye deni hakati tamaa kuweza kulipa deni lake lilio bakia ikiwa hana cha kumalizia hilo deni. Wala haianguki chini azma ya mujaahidi anaye pigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuinusuru Dini yake na kukomboa nchi yake kwa sababu ya kukosa mali ya kutimizia makusudio yake. Wala msafiri au mgeni mhitaji aliye mbali na mali yake hakosi wa kumkidhia haja zake kwa kumsaidia mpaka afike kwake. Na juu ya haya Zaka ilikuwa ni njia moja katika njia kubwa ulio chukua Uislamu kukombolea mateka na wafungwa na kuondoa utumwa. Na Uislamu umeongeza kutimiza malengo yake ya kijamii kwa ulimwengu mzima ikatupilia mbali chuki zinazo chusha za kidini, na ikatoa ruhusa Zaka wapewe makafiri ikihitajia haja kuwakopesha. Hali kadhaalika hupewa wale wanao itumikia Zaka, kama kuikusanya na kuigawa. Pia waandishi, na wasafiri, na wanao khasiri kwa ajili ya kupatanisha wenye kugombana, na wanao wasaidia Waislamu katika vita. Ama makusudio ya kiuchumi ya Zaka ni kuondoa ufakiri popote ulipo, na kumsaidia kila mwenye haja kama ilivyo kwisha tangulia.

23:5 - “Na ambao wanazilinda tupu zao, isipo kuwa kwa wake zao au kwa iliyo wamiliki mikono yao ya kulia. Kwani hao si wenye kulaumiwa. Lakini anaye taka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka.” Aya hizi zinaambatana na Aya nyengine ziliomo katika Suratun Nur zilizo anzia: “Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mpigeni kila mmoja wao bakora mia.” Hakika Aya hizi tukufu zilizo tajwa zinaashiria maovu ya katika umma yanayo tokea kwa uzinzi. Ama katika umma ni kuvurugika nasaba ya watoto isijuulikane, ama katika siha ni sehemu mbili. KWANZA ni katika mwili, mfano wa kisonono, tego, AIDS n.k. Kisonono huweza kuzalisha maradhi ya urithi kwa watoto hata huweza kuleta upofu. Ama tego (Syphilis) huenea katika mishipa ya damu na ya hisiya na huweza kuishia wazimu, na pia huenea mpaka kwa vizazi, na huenda mtoto akafa tumboni au akatoka na kilema. Ama maradhi ya AIDS (Ukimwi) hayo ni maafa yasiyo semeka, Mwenyezi Mungu atulinde nayo. PILI ni kuathirika mishipa ya hisiya na akili, kwani uzinzi huweza kuathiri dhamiri ya mtu, na kuadhibika nayo, na hata mwisho huweza kuingia wazimu.

23:6 - Zamani utumwa ulikuwa ni jambo la kawaida, na ilikuwa mtu akiweza kuchukua katika wajakazi wake akawafanya kuwa ni wakeze. Na Uislamu ulihalalisha utumwa wa mateka katika vita vilivyo fuata sharia ikiwa maadui nao wanakamata watumwa, basi ilikuwa ni halali kuwatendea wao hali kadhaalika. Ikiwa maadui hawawafanyi mateka kuwa ni watumwa basi ilikuwa haiwafalii Waislamu kuwafanya mateka kuwa ni watumwa.

23:17 - “Na kwa yakini tumeziumba juu yenu njia saba. Nasi hatukuwa wenye kughafilika na viumbe.” Hizo njia saba zilizo tajwa katika hiyo Aya maana yake ni mbingu saba, na kwamba hizo si mbingu moja, na Mwenyezi Mungu haghafiliki na

mbingu hizo na viumbe viliomo ndani yake.

23:18 - “Na tumeteremsha kutoka mbinguni maji kwa kiasi na tukayatuliza katika ardhi. Na hakika Sisi tunaweza kuyaondoa.” Aya hii tukufu inaashiria maana ya kisayansi yenye kukhusu mzunguko wa maji katika ardhi. Yajuulikana kuwa mvuke unao paa kutoka baharini hupelekea kufanyika mawingu ambayo ndiyo huteremsha mvua. Na hivyo ndio chanzo cha maji matamu juu ya uso wa ardhi, na ndio chombo cha msingi cha uhai wa ardhi. Kutokana na mvua ndio huzuka mito inayo zua uhai katika sehemu kamwe zisio pitikiwa na mvua. Kisha hiyo mito inamiminika baharini, na khulka inarejea tena kutoka baharini kwenda angani na kwendea nchi kavu, na kisha kuingia baharini mara ya pili. Isipo kuwa baadhi ya hayo maji ya mvua yanatulua na yanazama kuhifadhika katika mahodhi ya chini ya ardhi, yakawekeka kwa muda mrefu. Mfano wa hayo ni hayo maji yanayo patikana chini ya Jangwa la Magharibi katika Libya, ambayo yamegunduliwa na watafiti hivi karibuni kutokana na asli yake ya kale. Na huenda maji kama haya yalio hifadhika chini yakapatwa na mabadiliko ya joto wanayo yaita wataalamu wa ilimu ya t’abaka za ardhi (Geology) kuwa ni Mikondo ya Jiolojia, ikenda hiyo na maji mpaka pahala pengine pakavu, ikaleta uhai baada ya kuwa ni maiti.

Na Aya hii inaonyesha hikima kubwa ya uenezaji wa maji kwa kipimo, yaani kipimo cha haki na hikima, kwa ajili ya kuleta manufaa na kupinga madhara. Na tena maana nyengine ya Aya tukufu ni kufahamisha apendavyo Mwenye Kuumba, Aliye tukuka, navyo ni kujaalia yawepo maji ya kiasi maalumu katika bahari za ulimwengu kutosha kuwepo mizani ya joto la kufaa katika sayari hii, na ili isiwepo khitilafu kubwa mno baina ya joto la siku za joto, na baridi ya siku za baridi, hata ikawa ni muhali kubakia uhai, kama ilivyo katika sayari nyengine na katika mwezi. Kadhaalika maji ya ardhi yanateremka kwa kiasi maalumu, hayazidi yakafunika ardhi yote, wala hayatindikii sana hata yasipatikane hata kidogo kunyweshea baadhi ya nchi kavu.

23:20 - “Na mti utokao katika mlima wa Sinai, unatoa mafuta na kuwa kitoweo kwa walao.” Aya hii tukufu inathibitisha kuwa mti wa zaituni ni miongoni mwa neema alizo mneemesha Mwenyezi Mungu binaadamu na ambazo baadhi yake zimetajwa katika Aya zilizo tangulia. Na la kuongeza kwenye Aya hii ni kuwa mzaituni ni miongoni mwa miti ya mbao inayo ishi muda mrefu sana, zaidi ya mamia ya miaka. Kwa hivyo hauhitaji juhudi kubwa kwa mtu, bali huendelea kuzaa wenyewe mfululizo. Kadhaalika una sifa ya kuwa daima kijani, unapendeza kuutazama.

Uchunguzi wa kisayansi unaonyesha kwamba zaituni ni katika chakula kizuri. Kwani ndani yake imo Protein nyingi. Vile vile zimo chumvi za Calcium, chuma na Phosphorous. Na hivi ni muhimu na vya kutegemewa katika chakula cha binaadamu. Na juu ya hivyo zaituni inayo Vitamin A na Vitamin B. Na kutokana na tunda lake hutolewa mafuta ya zaituni, ambayo ni mafuta bora ya mafuta mepesi. Mafuta haya hutumiwa katika chakula. Uchunguzi wa kitabibu unaongeza kusema kuwa zipo faida nyengine katika mafuta ya zaituni, nazo ni kuwa zinasaidia kwa jumla katika viungo vya usagaji wa chakula, na khasa maini. Nayo yanashinda ubora mafuta yote yanayo tokana na mimea na wanyama, kwa kuwa hayasabibishi maradhi ya mishipa ya damu kama mafuta mengineyo, na kadhaalika yanalainisha ngozi. Na mafuta ya zaituni yana

matumizi mengine mengi katika sanaa (ufundi), kwani yanatumiwa katika kufanya sabuni nzuri kabisa, na vitu vinginevyo katika ufanyaji wa vyakula na vitu vya sanaa.

23:27 - “Tukampa wahyi: Unda jahazi mbele ya macho yetu na uwongozi wetu! Basi itapo fika amri yetu na ikafurika tanuri, hapo waingize ndani yake wa kila namna dume na jike, na ahali zako, isipo kuwa yule ambaye katika wao juu yake imekwisha tangulia kauli. Wala usinitajie hao walio dhulumu. Kwani hao bila ya shaka watazamishwa.” Hakika haya maelezo ya Tofani lilio tokea ijapo kuwa ni kwa mukhtasari tu katika hizi Aya tukufu, kwa mwenye akili ya kuzingatia yana maana na mambo ya hakika mengi ya ki-ilimu ambayo yanawapitia watu wengi. Na “tanuri” kwa lugha ni jiko la kuchomea mikate, au pia ni uso wa ardhi na kila chenye kutimbuka maji, na kila penye mkusanyiko wa maji.

Na si wepesi kusema kwa yakini taarikhi ya hiyo Tofani, kwani zilitokea tofani nyingi zama za kale, kama katika Babilonia, Bara Hindi na Amerika.

Na zipo baadhi ya hadithi za kienyeji mbali mbali zinazo taja khabari ya Tofani. Lakini haielekei kuwa hadithi hizo ndio zimekhusu hii Tofani kubwa au Tofani ya Nuhu. Uchunguzi umethibitisha na pia zimeonekana tofani nyingi ulimwenguni. Na tofani ya mwisho ya ulimwengu mzima ilikuwa sababu yake ni kumalizika kipindi cha barafu cha mwisho, na kuyayuka barafu nyingi ya kaskazini kabisa na kusini kabisa kwa dunia. Na sisi hatujui kwa yakini lini mizani iligeuka na tanuri ikafurika - yaani uso wa ardhi - kwa kupanda kwa ghafla kwa hivyo kuyayuka barafu, hata yakapanda juu maji ya bahari na ya kamwagika maji.

Yafaa kutaja kuwa kuyayuka barafu ya zama za barafu za mwisho kulileta hali ya hewa yenye mvua nyingi sana katika sehemu za dunia zililo mbali na huko kaskazini na kusini kabisa kwa ulimwengu, kama vile katika Bahari ya Kati (Meditereanian).

Vyo vyote vile ilivyo inakubalika kuwa hatuna ushahidi wa kuweza kusema lini khasa zilikuwa hizo zama za Nuhu na kaumu yake. Yaliyo dhaahiri kuwa yote hayo ni muujiza wa Mwenyezi Mungu. Na katika miujiza ni kuwa Nuhu aliwanasihia watu wake na akawaonya na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu akafunua kuwa atawazamisha ikiwa hawakutengenea. Na tena akamfunulia aunde marikebu. Kisha ikaja amri ya Mwenyezi Mungu, na mizani ikapinduka, na tanuri ikafurika, ikamiminika mvua kuthibitisha aliyo yasema Mwenyezi Mungu kumwambia Nuhu ya kwamba Mwenyezi Mungu anajua kuwa hatoamini mtu katika kaumu yake baada ya wale walio kwisha amini.

23:71 - “Na lau kuwa Haki ingeli fuata matamano yao, basi zingeli haribika mbingu na ardhi na waliomo ndani. Bali tumewaletea ukumbusho wao, nao wanajitenga mbali na ukumbusho wao.” Hilo neno “Haki” ni tamko lenye maana kadhaa. Huweza kuwa maana yake ni “Mwenyezi Mungu” Subhanahu wa Taa’la , mfano wa kauli yake Mtukufu: “Ametukuka Mwenyezi Mungu wa Haki”. Pengine huwa maana yake ni “Qur’ani” , kwa mfano :”Hakika Sisi tumekutuma kwa Haki”. Na huenda kukusudiwa “Dini yote”, yaani miongoni mwake ni Qur’ani na Sunna (Hadithi) Sahihi, mfano wa kauli yake: “Na sema: Imekuja Haki na uwongo umetoweka”. Na iliyo dhaahiri katika tamko la Haki hapa ni kuwa makusudio yake ni ile maana ya kwanza, yaani “Mwenyezi Mungu” Aliye takasika na kutukuka. Na kwa hivyo maana iliyo kusudiwa

Maelezo

na Aya ni: Lau kuwa mwenendo wa Mwenyezi Mungu unafuatana na watakayo na wanayo yapendekeza makafiri mpango usingeli bakia katika hali iliyo simamia shani ya mpango wa mbingu na ardhi na wa viumbe viliomo ndani yake. Lakini Mwenyezi Mungu Mwenye hikima kuu na uwezo wa kutenda na ujuzi wake ulio enea kwa viumbe vyake na hikima yake ikadhamini kwa mpango madhubuti, na Qur’ani kusema kwa uwazi ya kwamba mbingu zina viumbe, anataelekeza tufahamu:

- Kwanza kuwa Kuamini hayo kwa jumla ni yakini, tuache tafsili yake mpaka apendavyo Mwenyezi Mungu Subhanahu kuidhihirisha kwa kuambatana na kauli yake: “Tutawaonyesha Ishara zetu angani na katika nafsi zao.”
- Pili: Anataelekeza kwenye utafiti wa kisayansi kama tunaweza “kwani kufikilia hakika hii inatutilia nguvu Imani yetu. Na Imani ndiyo lengo muhimu katika kuelekea kwetu kwenye Ishara hizo.”

23:80 - “Na Yeye ndiye anaye huisha na kufisha, na yake Yeye mabadiliko ya usiku na mchana. Basi je! Hamfahamu?” Aya zenye kutaja usiku na mchana zimekuja mwahala mwingi katika Qur’ani tukufu, na haya yanaonyesha kuwa Mwenyezi Mungu wa Haki, Aliye takasika na kutukuka, anawakumbusha waja wake kwa Ishara hii ya uumbaji; na kwa kuwa yamo maana ya ndani inawapelekea wenye kufikiri wazidi kuzingatia na kuchungua. Na kukhitalifiana usiku na mchana kunatokana na pande mbili kubwa: Kwanza: Kukhitalifiana kwa wakati, urefu na ufupi. Na Pili: Kukhitalifiana kwa dhaahiri ya tabia na isiyo onekana.

* **Kwanza** - Khitilafu kwa nyakati:

Mchana ni kipindi cha wakati baina ya kudhihiri ncha ya jua na inapo potea upeo wa macho, pale linaponekana kwa jicho kama linagusa uso wa ardhi. Na ilivyo kuwa kwa hakika pale pahali pake pa kuzama jua sipo hapo upeo wa macho, bali tunaona tu hivyo kwa kuwa miale inayo tokana na jua inapinda inapo pita katika matabaka ya anga mpaka inapo fikilia kwenye jicho la mtazamaji, na yeye akalionga jua kama lipo huko upeo wa macho. Lilio kweli ni kuwa kuzama huku kuko chini kuliko upeo wa macho kwa kadri ya dakika 35 kwa kipimo cha mduara.

Na Usiku ni kipindi cha kutimiliza wakati wa mchana mpaka kitimilie kipindi cha mzunguko wa ardhi juu ya nafsi yake kutoka magharibi kwendea mashariki. Na baina ya Usiku na Mchana vipo vipindi viwili, navyo vya magharibi na mapambazuko. Na kipindi cha mchana kinakhitalifiana kwa mujibu wa hali ya uwazi wa pahala na musimu wa mwaka. Hali kadhaalika kipindi cha usiku kinakhitalifiana hivyo hivyo kwa kufuatana haya. Na nyakati za Sala na Saumu zinawekwa kufuatana na matulio ya jua huko upeo wa macho.

* **Pili** - Khitilafu katika yanayo dhihiri katika tabia:

Na madhaahiri haya ni ya namna nyingi, na yanazalikana kutokana na michanganyiko ya miale ya jua, inayo onekana na isiyo onekana, na vitu vilio beba nguvu za umeme pamoja na vifuniko vya anga na nyuso za bahari na majangwa n.k. Kadhaalika yapo mambo ya kuonekana kama kupatwa kwa jua na mwezi, na nyota zenye kufanya mikia, nyota za dasturi na nyota zierendazo na mawingu meupe, na nyota zinazo anguka, na ambazo hufumbwa na ukali wa anga la jua kuonekana mchana, ilhali usiku huonekana wazi. Na muhimu kabisa katika yanayo onekana kuwa ni khitilafu baina ya usiku

na mchana ni huu mwangaza wa mchana. Na sababu yake ni kuwa miale inayo toka kwenye jua inapo piga juu ya funiko la anga, ambalo kwa hakika ni sehemu ndogo ndogo zenye chembe chembe ndogo mno za vumbi, hizo hurejesha mwangaza na kuutawanya pande mbali mbali. Ikiwa hali ya anga ni safi, na vile vichembe chembe vya vumbi ni vidogo sana, na jua liko upeo wa macho, basi rangi inayo enea zaidi na inayo onekana kwa macho zaidi, inakuwa ya kibuluu. Ama wakati wa kuchomoza jua au kuchwa basi mbingu huonekana na rangi ya machungwa yenye kupiga wekundu, na mwangu wa kibuluu unatawanyika. Nz kwa hivyo mbingu utosini huelekea kuwa kibuluu khafifu.

Na wakati wa kuchwa jua tunaona rangi ya kijani kiasi ya nukta moja hivi au akali pembezoni mwake. Huu huitwa mmetuko wa kijani, na aghlabu yake huonekana unapo kuwa baharini, au nyuma ya kilele cha mlima, au hata kwenye kuta za majumba. Na asli ya kuonekana hivi ni kwa ajili ya kugeuka na kutawanyika miale ya jua hata ikatoa rangi mbali mbali katika hizo kijani.

Mukhtasari wa haya ni kuwa miale ya jua ina rangi zinazo onekana na zisizo onekana. Na zinakhitalifiana kwa urefu wa mawimbi yake na kufuata kwake sifa hiyo. Kwa hivyo ndio tunaona kwa migongano hiyo mwangaza wa mchana, mazigazi (sarabi), upinde wa mvua, na rangi za aina mbali mbali zinazo zunguka jua, na mengineyo katika Ishara za mbinguni za ulimwengu tuonao. Na linapo potea jua jioni mbingu inaonekana kwa rangi mbali mbali kwa sababu ya kuparaganyika mwangaza katika matabaka ya anga la juu. Na kila jua likiteremka unapungua mwangaza wa jioni, na zinapungua zile rangi zake za tabia, mpaka likifikilia daraja ya duara 18.5 mbingu inakuwa kiza. Na wataalamu wa nyakati wameweka kuwa huu ndio wakati wa kuambiwa kuwa usiku umekuwa giza na kwa hivyo ndio wakati wa kuadhinia Sala ya Isha. Na wakati huo khasa ndio huanza mwangaza wa nyota kama sura ya mnara wa sukari na tako lake liko upeo wa magharibi. Na hivyo huendelea katika masiku safi ya siku za baridi mpaka kilele cha ile “cone” au “makhrut” yaani sura ya mnara wa sukari kifikie utosini. Na kati kati ya usiku hudhihiri rangi za kuchomoza jua kidogo kidogo wakati wa mapambazuko kwanza kama kilele cha ile “cone” au “makhrut”. Kilele chake hicho huzidi kupanda, na tako lake hutanuka kwenye upeo wa mashariki mpaka inapo dhihiri alfajiri, yaani linapo kuwa jua liko chini ya upeo wa macho wa mashariki kwa kadri ya daraja 18.5 za duara. Na hapo ndio wakati wa kuadhiniwa Sala ya Alfajiri. Na rangi za mapambazuko huanza kudhihiri kwa taratibu kinyume na zile za kuchwea jua magharibi. Na imedhihiri karibuni kuwa jua lina kifuniko chembamba kimetanda angani takriban kimekaribia kufunika anga lote la ardhi. Kifuniko hichi chembemba ndicho kinacho sabibisha kuleta rangi mbali mbali za katika anga.

Mambo haya mbali mbali ambayo tumeyataja kama ni mifano isiyo na ukomo imetuonyesha vipi mbingu inavyo kuwa pindi ikiwa hapana mawingu wala hapana pepo za mchanga. Kwani hapo tena huwa ni kiza. Na ikiwa mawingu yamebeba matone ya maji ya mvua basi hayo hupambana na miale ya jua, na hufanyika kama huo upinde wa mvua katika hali maalumu.

Na ikiwa mawingu yenyewe ni ya namna fulani ambayo yanabeba maji yaliyo ganda (crystals) “kristali” zenye pande sita, basi maji hayo huingiana na miale ya jua na hiyo miale huvunjika ndani ya hayo maji (kama mwaangaza upitavyo katika kigae cha thuraya, “prism”) kisha mwangaza huo ukatoka nje kwa rangi mbali mbali. Na katika

hali fulani fulani ndio hutokea rangi nzuri nzuri kulizunguka jua. Na wakati wa weusi wa usiku utazona nyota kama kwamba zipo karibu nasi na kwa hakika hizo ziko mbali kwa masafa makubwa sana ya kukisiwa kwa miaka na miaka ya mwendo wa mwanga. Vile vile tunaona katika anga hili nyota na sayari na nyota mkia na vimondo kama kwamba zipo karibu, utadhani kuwa khitilafu ya masafa imeondoka kabisa. Na haya ndiyo yanayo tupelekea tutambue maana iliyo fichikana ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Na tumeifanya mbingu kama dari iliyo hifadhiwa; nao wamezipuza Ishara zetu.” Kama tulivyo kwisha eleza kuwa juu ya miale inayo tokana na jua kuna miale inayo tokana na vitu vingine vya eneo la jua vyenye nishat’i ya nguvu, na vyenye kubeba nguvu za umeme. Kadhaalika inatokana na hizo miale iliyo juu ya zambarau Ultra Violet Rays. Vitu hivi na miale hii inapambana na matabaka ya anga la juu, na huathirika kwa mvuto wa smaku kuizunguka dunia. Kwa hivyo hilitibua anga la kaskazini na kusini, na huleta kiza katika mbingu ya kaskaazini kama kwamba ni pazia kuzuia mianga yenye rangi nzuri nzuri za kijani zenye kumili kwenye wekundu na kibuluu. Sura hizi hubaki pengine muda wa saa kadhaa katika mbingu ya kaskazini, na zaidi waweza kuziona masiku kadhaa wa kadhaa linapo kuwa jua linashitadi. Mapazia haya si kama unayaona kaskazini tu, bali hata pia katika kati kati ya dunia.

Na katika mbingu vipo vibebaji nguvu za umeme katika mawingu na anga ambavyo huzalikana kutokana navyo radi na mimetuko katika anga la juu. Mambo yote haya yanayo onekana ambayo tunayashuhudia yanatupelekea tufahama maana ya ndani ya kauli yake Subhanahu wa Taa’la: “Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi na kukhitalifana usiku na mchana pana Ishara kwa wenye akili.”

Kutokana na yaliyo pita kwa mambo ya dhaahiri ya maumbile inabainikana kwamba haya yanakuwa kwa sababu ambazo hayumkini mwanaadamu kuingilia ndani yake. Na hakika ni Mwenyezi Mungu, Aliye tukuka shani yake, ndiye mwenye kuleta hizo khitilafu za usiku na mchana, wala hawezi binaadamu kabisa siku yoyote kuweza kugeuza usiku wala mchana. Na Yeye Mwenyezi Mungu Aliye tukuka shani yake ndiye anaye zifuatanisha usiku na mchana kwa mizani madhubuti na vipimo baraabara, na anaendesha siku zote mwaka ingia mwaka toka.

24:3 - Haya ikiwa haikupita toba. Na tafsiri ya haya ni kuwa inabainishwa tabia za washirikina au wazinifu kuwa wao hawapendi ila mambo ya ufisadi tu. Na kwa mujibu wa maoni ya Hambali na Ahli-Dhaahir (na pia Ibadhi) haisihi ndoa ya mwanamume mzinifu au mwanamke mzinifu kabla ya toba.

24:4 - Maoni ya Wataalamu juu ya Aya 2 - 4:

“ Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mtandikeni kila mmoja katika wao bakora mia. Wala isikushikeni huruma kwa ajili yao katika hukumu ya Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na lishuhudie adhabu yao kundi la Waumini. Mwanamume mzinifu hamwoi ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina. Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mshirikina. Na hayo yameharimishwa kwa Waumini. Na wanao wasingizia wanawake mahashumu, kisha wasilete mashahidi wane, basi watandikeni bakora thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena. Na hao ndio wapotovu.” Makosa katika Sharia ya Kiislamu ni mambo yaliyo harimishwa na Mwenyezi Mungu akayakemea

kwa kuyawekea adhabu au izara ya kufedhehesha. Na maharimishwa hayo ama ni kutenda kilicho katazwa kukitenda, au kuacha kutenda kilicho amrishwa na Sharia kutendwa. Na sababu ya kuharimishwa haya yaliyo katazwa ni kuwa hayo ni kupiga vita moja katika maslaha yanayo kubaliwa katika Uislamu. Na maslaha hayo yanayo kubaliwa ni matano, nayo ni:

1. Kuhifadhi nafsi.
2. Kuhifadhi Dini.
3. Kuhifadhi akili.
4. Kuhifadhi mali
5. Kuhifadhi hishima.

Kuuwa kwa mfano ni kuipiga vita nafsi. Na kurtadi, kutoka katika Uislamu, ni kuipiga vita Dini. Na kutumia vinavyo levya ni kuipiga vita akili. Na wizi ni kuyapiga vita mali. Na uzinzi ni kuipiga vita hishima.

Na wanazuoni wa ilimu ya *Fiqhi* (Sharia) wameyagawa makosa sehemu mbali mbali. Lakini sisi yatutosha kwa sababu ya kueleza Aya hizi kugawa kwa mujibu wa uzito wa adhabu zake, na namna ya kiasi chake. Nayo yamegawika mafungu matatu:

1. H'udud, yaani Adhabu.
2. Kisasi au Diya
3. Izara, au Fedheha.

Ama H'udud, au Adhabu, ni makosa ambayo yanaonekana kuwa yanaingilia kuvunja Haki ya Mwenyezi Mungu, au kuwa Haki ya Mwenyezi Mungu ni kubwa zaidi ndani yake kuliko haki ya binaadamu. Na kwa hivyo ndio Mwenyezi Mungu akaiwekea MIPAKA ndio maana khasa ya H'udud. Kaiwekea mipaka adhabu yake katika Qur'ani au katika Sunna za Mtume s.a.w. Ama makosa ya Kisasi na Diya ni makosa ambayo baadhi kubwa yake yamewakhusu wenyewe waja. Mwenyezi Mungu amewekea adhabu za baadhi yake katika Qur'ani au katika Sunna za Mtume s.a.w., na amewaachilia mengine wapime wenyewe wenye madaraka. Mfano wa hayo makosa ya kumwaga damu, kama kuuwa na kukata viungo, na kujuruhu.

Ama makosa ya Izara, Uislamu umejitosheleza kwa kutaja mwisho wa ukali na mwisho wa upole katika adhabu zao, na kuachia yaliyo baki wenye kutawala wahukumie kwa kila kosa kwa mujibu wa hali na zama yanapo tokea makosa.

Makosa ya H'udud ni saba:

1. Uzinzi.
2. Kuzulia wanawake mahashumu wasio na makosa.
3. Udhhalimu.
4. Wizi.
5. Uharamia.
6. Ulevi.
7. Kurtadi. (Kutoka katika Uislamu).

Mwenyezi Mungu ameyawekea mipaka yote makosa hayo na ameyaleta kwa hisabu yake katika Qur'ani, kama alivyo wekea adhabu zake katika Qur'ani vile vile, isipo kuwa adhabu ya mwenye kuzini naye amewahi kuo, yaani *Zaani Muh's'an*, ambaye hupigwa mawe, na mlevi na adhabu yake ni fimbo thamanini, na adhabu ya mwenye kurtadi ambaye jaza yake ni kuuwawa. Hayo yamekuja katika Sunna.

Na zimezoea hizi kanuni za kuundwa na watu katika kupinga makosa ya uzinzi kwa adhabu khafifu kama vile kifungo, hata ndio uchafu ukaenea kati ya watu, na fiski na ukahaba ukazagaa, na hishima zikapotea, na maradhi yakakithiri, na nasaba za ukoo zikachanganyika. Katika jambo la ajabu ni kuwa hizi kanuni za kisasa za nchi zinazo ambiwa za kistaarabu ndio zinazo yalinda makosa haya. Katika kanuni za adhabu za Kifaransa, kwa mfano, wazinzi wasio oa wala kuolewa hawapati adhabu yoyote

maadamu wao wakiwa wamekwisha fikilia utu uzima. Kwa kuwa ati uhuru wao wa binafsi unataka waachiliwe wajifanyie wenyewe watakalo. Ama mzinzi mwanamume aliye na mke, au mwanamke mwenye mume, basi huyo adhabu yake ni kifungo. Lakini mwana sharia wa serikali haingii kuchunguza ila akipata mashtaka kutokana na mume au mke. Na inaonyesha kuwa ni haki ya mume tu kuwa hilo kosa limetokea au la, kwani ikiwa yeye ndiye aliye fikisha mashtaka, basi yeye anaweza kuyafuta pia, na uchunguzi utasita. Na yeye anaweza kumsamehe mkewe akatoka gerezani kabla ya kutimiza muda wa kifungo chake ijapo kuwa hukumu ilikuwa ni juu yake huyo mwanamke mwishoni.

Na wapo baadhi ambao ati wanaushutumu Uislamu kwa ukali wake kushadidia kwake kuadhibiwa wazinifu. Yaliyo elekea zaidi ni kuwa lau wangeli zingatia kuwa kama ilivyo kuwa adhabu ni kali, hali kadhaalika umeshadidiwa ushahidi kwa jambo hili. Kwani ijapo kuwa katika kosa la mauwaji yatosha ushahidi wa mashahidi wawili waadilifu, katika uzinzi ni lazima wapatikane mashahidi wane waadilifu walio ona kitendo hicho kwa macho yao, au aungame mkosa!

Hayo, na tunaona kuwa Qur'ani Tukufu imelazimisha kuwa kupigwa hizo fimo kuwe jahara ili mkosa ajuulikane, na iwe ni onyo kuwakhofisha wenginewe.

24:22 - Aya hii imeteremka pale Abu Bakar r.a. alipo apa kumkatia msaada jamaa yake Mist'ah bin Uthaathah hapo alipo ingia Mist'ah katika uzushi alio zuliwa bibi Aisha r.a.

24:33 - Haya yanaelezwa na kauli ya Mtume s.a.w.: “Enyi vijana! mwenye kuweza kuwoa na aoe kwani hivyo linalindwa jicho, unahifadhiwa utupu. Asiye weza na afunge, kwani hivyo ni kinga yake.”

24:40 - “Na walio kufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji. Hata akiyaendea hapati chochote. Na atamkuta Mwenyezi Mungu hapo naye amlipe hisabu yake sawa sawa. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.” Sarabi si chochote ila mandhari ya mwangaza yanayo sabibishwa na marejeo (reflection) ya miale inayo toka kwenye vitu vyenye kutoa mwanga. Na hiyo hurejeshwa tena kutokana na ardhi pana tupu, yaani uwanda, na kupanda kidogo kidogo mkabala na uso wa ardhi, na joto linapo panda wakati wa mchana, basi miale hiyo inayo rejea ikifika kwa jicho la mwenye kuangalia huona vile vitu vimegeuka juu chini kama kwamba kwenye kiyoo kikubwa kilicho tanda. Na kadhaalika mbingu safi ya rangi ya kibuluu huonekana kama kwamba ni ziwa la maji juu ya uso wa ardhi. Na vile vitu vingine kama miti miti na mitende iliyo onekana juu chini inazidi kuonyesha kama kwamba ni vivuli kwenye maji. Na hii Sarabi huzidi kudhihiri kwa uwazi kabisa inapo kuwa khitilafu ni kubwa baina ya joto la uso wa ardhi na angani katika hewa. Na hayo huonekana zaidi majangwani na nyandani na kwenye barabara za jangwani za lami zililo nyooka. Kwa maelezo hayo inaonekana kuwa Sarabi ni kiini macho tu.

Maoni ya wataalamu juu ya Aya 40:

“ Au ni kama giza katika bahari kuu, iliyo funikwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu. Giza juu ya giza. Akiutoa mtu mkono wake anakaribia

Maelezo

asiuone. Na ambaye Mwenyezi Mungu hakumjaalia kuwa na nuru hawi na nuru.” Aya hii tukufu imekusanya yaliyo muhimu kabisa katika midharuba ya baharini. Ni maarufu kuwa midharuba ya bahari kuu huwa na mawimbi yanayo khitalifiana urefu wao na ukubwa wao au mnyanyuko wao, hata inaonekana kama kwamba hayo mawimbi yanapandana moja juu ya mwenzie, na kwa hivyo yakaziba mwangaza wa jua kwa vile hiyo midharuba inasabibisha kurundika kwa mawingu mazito ambayo nayo huuziba mwangaza wa jua, na kwa hivyo husabibisha giza mtu asiweze kuona kitu juu ya kuwa macho yake mazima. Na ilivyo kuwa Mtume s.a.w. kazaliwa na kakulia jangwani, kuja maelezo kama haya ya undani ya ki-ilimu kwa ulimi wake kuwa ni ufunuo ulio tokana na Mwenyezi Mungu, ni ushahidi kuwa Qur’ani inatoka kwa Mwenyezi Mungu, na kuwa ni muujiza wa Mtume huyu mtukufu.

24:43 - (1) Hajui kushabihiana baina ya mawingu na milima ila mwenye kupanda ndege (eroplani) inayo ruka juu ya mawingu, akayaona kutoka huko juu kama ni milima na vilima. Ilivyo kuwa ndege hizo hazijawa bado zama za Mtume s.a.w. basi hii inakuwa ni dalili kuwa maneno haya yanatokana na Mwenyezi Mungu anaye jua ya juu na chini.

(2) “Je! Huoni ya kwamba Mwenyezi Mungu huyasukuma mawingu, kisha huyaambatisha, kisha huyafanya mirundi? Basi utaona mvua ikitoka kati yake. Na huteremsha kutoka juu kwenye milima ya mawingu mvua ya mawe, akamsibu nayo amtakaye na akamuepusha nayo amtakaye. Hukurubia mmetuko wa umeme wake kupofua macho.” Aya hii tukufu imeutangulia msafara wa sayansi. Kwani hii yaeleza daraja za kuundika mawingu yanayo rindikana, na sifa zake, na yaliyo juulikana hivi karibuni ki-sayansi ya kwamba mawingu ya mvua huanzia kwa sura ya moja moja kisha yakajumuika yakawa kikundi, ndiyo hayo mawingu yaliyo rindikana, yaani mawingu yanayo endelea kukua kwa kuelekea utosini. Hayo hukua kimo chake hata kufikia urefu wa kilomita 15 au 20, na hapo huonekana kama ni milima mikubwa iliyo nyanyuka.

Na yajuulikanayo ki-sayansi ni kuwa mawingu yaliyo rindika yanapitia daraja tatu, nazo:

Daraja ya kukusanyika na kukua.

Daraja ya kunyesha.

Na mwisho daraja ya kumalizikia.

Kama ilivyo kuwa mawingu hayo - nayo ni peke yao - yenye mvua ya mawe na inabeba nguvu za umeme (electricity, Kahrabaa) , huweza kuwa yakashika mfululizo wa umeme na radi, hata huweza ikawa ni miripuko karibu 40 kwa dakika moja, hata mtu anaye tazama akawa hawezi tena kuona kwa ukali wa mwanga wake. Na haya ndiyo khasa yanayo wapata marubani wa meli na ndege wakati wa midharuba ya radi.

24:45 - “Na Mwenyezi Mungu ameumba kila kinyama kutokana na maji. Wengine katika wao huenda kwa matumbo yao, na wengine huenda kwa miguu miwili, na wengine huenda kwa miguu mine. Mwenyezi Mungu huumba ayatakayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.” Maji katika Aya hii tukufu ni maji ya

uzazi, yaani vinyama vinavyo toa manii. Na Aya hii si kama imetangulia msafara wa sayansi katika kubainisha kuzalikana mtu kutokana na tone la manii, kama ilivyo kuja katika kauli yake Aliye tukuka: “Hebu naajitazame mtu, ameumbwa kwa kitu gani? Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa.” (Sura Att’aariq 5-6), bali imetangulia pia katika kubainisha kwamba kila kinyama kinacho kwenda kwenye ardhi kimeumbwa kwa njia ya kuzalikana na vinyama vya manii, na vinga khitalifiana hivyo vinyama vya manii na sifa zao katika kila namna mnamo hizo namna za vinyama. Katika maana za kisayansi ambazo zaweza kuwa nazo hii Aya ni kuwa maji ni msingi wa kila kiumbe kilicho hai. Kwa mfano mwili wa mtu umekusanya 70% ya uzito wake kuwa ni maji. Yaani mtu mwenye uzito wa kilo 70, kiasi kilo 50 ni maji. Na kabla ya kuteremka Qur’ani haya hayakuwa yakijuulikana kabisa ya kuwa mtu ana sehemu hii kubwa ya mwili wake kuwa ni maji.

Na maji ndio chakula cha dharura kabisa kwa mwanaadamu. Kwani hali mtu yamkini aishi siku 60 bila ya kula chakula chochote, hawezi kuishi bila ya maji kwa zaidi kuliko siku 3 mpaka 10 mwisho wake.

Na maji ndio msingi wa kufanyika damu, na maji ya limfo, na ya katika ubongo wa mifupa, vimwagavyo na mwili, kama mkojo, na jasho, na machozi, na mate, na nyongo, na maziwa, na maji yanayo patikana katika viungo, na ambayo ndiyo sababu ya ulaini wa mwili. Na yakikosekana 20% ya maji yake basi mwanaadamu hukabiliwa na mauti.

Na maji huyayusha vyakula vikasahilika kufyonzeka. Na kadhaalika huyayusha makombo yenye asili ya vilivyo hai au maadini katika mkojo na jasho. Na kwa namna hii maji yana sehemu kubwa zaidi na muhimu kabisa katika kuumbwa kwa mwili. Na kwa hivyo yamkini kusema kwamba kila kiumbe kilicho hai kimeumbwa kutokana na maji.

24:58 - “Enyi mlio amini! Nawakutakeni idhini iliyo wamiliki mikono yenu ya kulia na walio bado kubaalighi miongoni mwenu mara tatu - kabla ya Sala ya alfajiri, na wakati mnapo vua nguo zenu aduhuri, na baada ya Sala ya isha. Hizi ni nyakati tatu za faragha kwenu. Si vibaya kwenu wala kwao baada ya nyakati hizi, kuzungukiana nyinyi kwa nyinyi. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo kuelezeni Aya zake, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.” Aya hii tukufu ni moja katika Aya zinazo elekeza nadhari ya watu wazingatie yaliyo laiki katika jamii za watu khasa ndani ya ukoo. Nayo kuwa kuchanganyika kwa watumishi na watoto katika aila yao huenda kukapindukia mipaka ya hishima za maingiano, wakawa wanawaingilia wenginewe bila ya kutaka idhini katika nyakati maalumu zilizo tajwa katika Aya. Na kwa kuwa nyakati hizo ni nyakati za faragha na uhuru wa binafsi, na kuvua nguo nzito nzito, Aya hii imekusudia kuweka Sharia ya kutaka idhini katika nyakati hizo kutokana na watumishi na vijana ili wasione ambayo yanahisabiwa kuwa ni siri, ambayo ni kama utupu ambao wapasa kusitiriwa. Na kwa hivyo wanaelekezwa watu wa ukoo wavae mavazi yanayo kuwa laiki ya kukabiliwa hata wao kwa wao, ili hishima yao ibaki imehifadhika, na uhuru wao umedhaminika, na adabu zao zimechungika. Na Qur’ani ndio inaayo faa khasa kutuongoza tufuate mwendo ulio bora na wa juu. (Ikiwa watoto wa nyumbani haiwafalii kuwaingilia watu katika nyakati hizo za faragha zilizo tajwa,

seuze watu mbali!)

25:2 - “Ambaye ni wake ufalme wa mbingu na ardhi, wala hakuwa na mwana, wala hakuwa na mshirika katika ufalme, na akaumba kila kitu na akakikadiria kwa kipimo.” Ilimu ya sayansi ya sasa imethibitisha kuwa vitu vyote vinakwenda kwa mujibu wa hukumu za uumbaji wake, na maendeleo yake namna mbali mbali kwa kufuata mpango madhubuti ambao hapana mwenye uwezo juu yake ila Muumbaji mwenye uwezo Mwenye kuanzisha kila kitu. Kwani katika kuwa kwake imebainika kuwa vitu vyote viumbe vyote na vinga khitalifiana umbo lake na sura yake kwa hakika vinatokana na madda chache za asli za kuhisabika, na hisabu ya madda hizo (elements) zinakaribia mia, nazo ni 96 zinazo juulikana mpaka sasa. Nazo zina khitalifiana kwa sifa zao za maumbile (physically) na za Al Kimyaa (Chemically), na pia katika uzito wake wa chembe (Atomic Weight). Zinaanza kwa madda asli (element) Nambari 1. Nayo ni Hydrogen yenye Atomic weight 1, na kuishia na element ya nambari 96, Borium, ambayo atomic weight yake bado haijuulikani. Na element ya mwisho katika sayansi ni Uranium na atomic weight yake ni 238.57. Na hizi elements hujengeka na kufanyika Compounds kwa mujibu wa kanuni madhubuti zisio weza kuepukwa. Hali kadhaalika mimea na wanyama. Kila mmoja wao amegawika katika koo na makundi na namna (orders, families, species and sub-species) zinazo geuka sifa zake kwa madaraja ya viumbe vilivyo hai mpaka kuishia viumbe vyenye Khalaya au Cell moja (unicellular) kama microbes mpaka viumbe vyenye cells nyingi (multi- cellular) mpaka kufikia binaadamu, naye ndiye aliye kamilika kuliko wote. Na kila namna ya hizi sifa maalumu zinarithika katika kundi kizazi baada ya kizazi. Na yote haya yanakwenda kufuata kanuni na mipango iliyo thibiti madhubuti inayo onyesha kwa uwazi utukufu wa Mwenye kuumba na uwezo wake. Ametakasika, Subhanahu na ametukuka na hao wanao mshirikisha naye.

25:38 - Rass, kama ilivyo elezwa katika *Mufradaat ya Raaghib Al-As'fahani*, ni bonde, na akatolea ushahidi ubeti wa shairi: (Nao ni bonde la Rass, kama mkono kwa mdomo.) Hao watu wa Rass, kama ilivyo kuja katika Aya tukufu, ni watu walio kuwa wakiabudu masanamu. Mwenyezi Mungu aliwatumia Shuaib. Basi hao ndio walio pelekewa Mtume Shuaib a.s. Na Mwenyezi Mungu Aliye takasika amewaeleza hao kaumu ya Shuaib kuwa ni Watu wa Vichakani (Al-Aykat), napo ni pahali penye miti mingi panasifika kwa neema, na mara nyengine wanaitwa Watu wa Rass, nalo ni bonde lenye kheri kubwa, kuonesha neema alizo waneemesha Mwenyezi Mungu. Nao wakazikufuru neema za Mwenyezi Mungu, wakaabudu masanamu.

25:45 - “ Je! Huoni jinsi Mola wako Mlezi anavyo kitandaza kivuli. Na angeli taka angeli kifanya kikatulia tu. Kisha tumelifanya jua kuwa ni kiongozi wake.” Aya hii inadhahirisha hima ya Muumba na uwezo wake. Kwani kutandaza kivuli kunaonyesha mzunguko wa dunia na kuinama kwa msumari-kati (axis) wake. Na lau kuwa ardhi, yaani dunia, ingeli tulia tu, haitaharaki kulizunguka jua, na pia ikawa haizunguki wenyewe kwa wenyewe juu ya msumari-kati wake, basi kivuli kingeli tulia, na mwako wa jua ungeli piga juu ya nusu ya dunia, na nusu ya pili ikabaki ni usiku, moja kwa moja. Hayo yangeli leta khitalafu kubwa za baridi na joto, na ingeli pelekea kutoweka

uhai kabisa katika dunia. Na kadhaalika ingeli kuwa hii ni hali ya dunia basi kivuli kingeli tulia. Na haya pia yange tokea ikiwa muda wa kuzunguka ardhi juu ya msumarikati wake ndio muda ule ule muda wa kuzunguka kwake kulizunguka jua, yaani siku moja ikawa sawa na mwaka mzima. Lakini hapana awezaye kufanya hayo isipo kuwa Mwenyezi Mungu. Haya licha ya kuwa kivuli nafsi yake ni neema miongoni mwa neema za Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu aliviumba vitu vyote vyapenyeza mwangaza (transparent) kisingeli kuwapo kivuli, na vitu visingeli pata fursa ya kuwepo ambavyo vinahitajia vivuli.

25:48 - “Na tunayateremsha kutoka mbinguni maji safi.” Katika Aya hii tukufu Mwenyezi Mungu anawasimbulia watu kwa kuwateremshia maji yaliyo safi kutoka mbinguni. Na Aya hii inafahamisha kuwa maji ya mvua katika asili ya kuumbwa kwake ni maji safi kabisa. Na juu ya kuwa baada yake yanabeba takataka nyingi katika anga, lakini bado yamo katika daraja ya usafi.

25:53 - “Naye ndiye aliye zipeleka bahari mbili, hii tamu mno, na hii ya chumvi chungu. Na akaweka baina yao kinga na kizuizi kizuicho.” Yamkini Aya hii inaashiria neema ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake kwa kuto changanyika maji ya chumvi yanayo penya kutoka baharini kwenye miamba ya karibu na mwambao, na maji matamu yanayo penya kutoka bara, yasichanganyike kwa ukamilifu na hali nayo yanakutana. Matamu yanakuwa yako juu ya maji chumvi kama kwamba baina yao pana kinga kinacho zuia haya yasiingiane na haya, na kizuizi kizuicho, yaani kizuizi chembamba tusicho weza kukiona. Na haya si tu, bali ipo kanuni madhubuti inayo hukumu makhusiano haya, na inayo yahukumu kwa maslaha ya wanaadamu wanao kaa katika maeneo hayo, na maisha yao yanategemea kuwepo hayo maji matamu. Kwani imethibiti kuwa t’abaka ya maji matamu yalioko juu huzidi unene wake kwa mujibu wa kuzidi usawa (level) wa bahari kwa mpango maalumu. Hata inakuwa yawezekana kuhisabu kina cha mwisho cha maji matamu ambayo yamkinika kuyapata. Kwani hiyo ni sawa sawa na kadri ya khitilafu baina ya usawa (level) wa ardhi na usawa wa bahari mara arubaini.

25:59 - “Ambaye ameziumba mbingu na ardhi, na viliomo ndani yake kwa siku sita. Kisha akatawala juu ya A’rshi, Arrahman, Mwingi wa Rehema! Ulize khabari zake kwa wamjuaye.” Hizo Siku Sita ni usemi wa Mwenyezi Mungu, Mtukufu Aliye tukuka, kueleza wakati. Na Yeye Mtukufu ndiye Mwenye kujua zaidi kipimo cha hiyo Siku. Na kwa upande wa kiilimu za sayansi kazi ya kuumba ulimwengu unahitaji kupita vipindi na viwango mbali mbali. Na “Mbingu na ardhi na viliomo ndani yake” ni ishara ya vyombo vyote vya mbinguni, nyota, majua, sayari, miezi, mavumbi, gesi za namna mbali mbali, na nishat’i, Energy, na vyote hivyo vinavyo fanya ndio ulimwengu wa duniani na angani. Na kwa kuupanga ulimwengu wote, yaani uumbaji wote, kwa tafsihi ya ukamilifu inayo kusanya kila kitu, ndio inaweka wazi, Utawala wa Mwenyezi Mungu, Subhanahu juu ya ulimwengu kwa jumla na kwa tafsihi. “Uliza khabari zake kwa ajuaye”. Katika kifungu hichi cha Aya hii tukufu pana uwongozi wa kisayansi kutokana na Mwenyezi Mungu kuonyesha dharura ya uchunguzi na utafiti wa mambo yanayo onekana ya uumbaji na mipango yake tuyaangalie ya ndani, ili tujue siri za uweza wa Mwenyezi Mungu katika kuanzisha huu ulimwengu.

25:61 - “Ametukuka aliye zijaalia nyota mbinguni, na akajaalia humo taa na mwezi unao ng’ara.” Aya hii tukufu inaashiria maana za ki-ilimu za sayansi zenye kukusanywa katika mpango wa ulimwengu alio uumba Mwenyezi Mungu, Aliye takasika, Aliye tukuka, na zikazidi fadhila zake. Na sisi tunashuhudia nyota za mbinguni kwa sura ya makundi ambayo takriban hayageuki sura na yangapitiliwa na karne, na Buruuj nayo ndio hayo makundi ya nyota, ni yale yale yanayo pitiwa mbele yake na jua katika mzunguko wake unavyo dhihiri kuizunguka ardhi. Hizo Buruuj ni kama vituo vya jua katika mzunguko wake katika mwaka. Na kila tatu katika hizo huwa ni musimu katika misimu ya mwaka. Nazo kwa kuzitaja moja moja kuanzia msimu wa Rabii’ (Spring) unao kuja baina ya siku za baridi na joto, ni kama ifuatavyo kwa majina ya Kiarabu na Kizungu: Alh’aml (Aries, or Ram), Ath-thawr (Taurus), Aljawzaa’ (Gemini), Assarat’aan (Cancer), Al Asad (Leo), Assunbulah (Spica), Al Miiizaan (Libra), Al-A’qrab (Scorpion), Al Jadyu (Capricorn), Addalwu (Aquarius), Alh’uut (Pisces). Na jua ni moja katika nyota zenye nguvu za kati na kati. Nalo kama nyota zilizo baki lina mwangaza wake mwenyewe wa dhati kwa vituko vya kichembechembe (atomic reaction) vinavyo tokea ndani yake. Basi miale ya jua inayo toka kwenye nguvu hizo huangukia juu ya sayari, na ardhi, na miezi, na vyombo vilio baki vya mbinguni ambavyo havina mwanga wa nafsi yao. Kwa hivyo navyo hutoa nuru. Basi jua ndio Taa inayo waka kwa nafsi yake. Ama mwezi unarudisha nuru ya mwanga wa jua kutokana na uso wake, kama kiyoo. Hakika kwa kusifiwa Jua kuwa ni Taa, na ukasifiwa mwezi kuwa unatoa nuru, ni ishara ya kuwa Jua ndio chanzo cha nguvu, nishati, (T’aaqah, Energy) za joto.

26:165 - “Je! Katika viumbe vyote mnawaingilia wanaume?” Yaani kazi ya liwat’i, ambayo tangu asli yake ni ukosefu muovu, unao chusha hata kuusikia, kinyume na maumbile, unao mteremsha mwanaadamu chini kabisa. Na lau kuwa unaenea basi huharibu sunna ya kuoa, nayo ni sunna ya maumbile, hata uzazi ukatike na ulimwengu usite kuendelea.

Na kwa liwat’i huenea maradhi kama yanavyo enea kwa uzinzi kama tego, kisonono, donda ndugu, maradhi ya ngozi kama ukurutu, na hutokea ishara za kudhoofika nyama za nyuma hata ikawa mtu hawezi kujizua kutokwa na choo ovyo. Na nyuma kwake mtu huchanua kukawa kama mdomo wa tarumbeta. Na huko nyuma hujaa vijidudu vya maradhi na hivyo humuambukiza mwenye kumingilia na yeye hivyo vijidudu vikenda mletea maradhi mengine ya njia za mkojo. Na huenda huyo mwenye kufanywa mambo hayo akawa mpumbavu hafai kitu, ikiwa kaanza tangu utotoni. Na huenda akajidai kuonesha ujanadume mwingi kuliko kiasi kwa kutaka kuficha upungufu wake wa uume. (Karibuni imedhihiri kuwa maradhi ya khatari kabisa ya AIDS [Ukimwi] yameenea zaidi sana kwa watendao kitendo hichi na watumiao madawa ya ulevi, ijapo kuwa na wazinzi nao hupata!).

Na Mwenyezi Mungu Subhanahu wa Taa’la ameukemea ukosefu huu katika Aya kadhaa wa kadhaa, na akabainisha hikima ya Mwenye kuhukumu kwa kuharimisha huku, kwa kusema: “ Je! Katika viumbe vyote mnawaingilia wanaume? Na mnaacha alichu kuumbieni Mola wenu Mlezi katika wake zenu? Ama kweli nyinyi ni watu mnao ruka mipaka!”

27:10 - Kisa cha Musa kimetajwa zaidi ya mara moja katika Qur’ani. Pengine hutolewa yasiyo tajwa penginepo. Na kila sehemu ina mnasaba wake. Katika sehemu hii makusudio ni kuondoa yale mastaajabu ya kuwa Nabii Muhammad s.a.w. kapata Ufunuoa (Wahyi) vile vile.

27:12 - Hizo Ishara tisa ni:- Kupasuka bahari, T’ufani (Kimbunga), Nzige, Chawa, Vyura, Damu, Ukame, Fimbo, Kutoka mkono mweupe bila ya maradhi.

27:16 - “Na Sulaiman alimrithi Daudi, na akasema: Enyi watu! Tumefunzwa usemi wa ndege, na tumepewa kila kitu. Hakika hii ni fadhila iliyo dhaahiri.” Sulaiman a.s. ni mwana wa Daudi, naye ni Nabii na Mfalme kama yeye. Aliishi mnamo mwaka 974 mpaka 937 K.K. (yaani Kabla ya Kuzaliwa Nabii Isa). Mwenyezi Mungu alimjaalia kumjuvya kufahamu maneno ya ndege. Uchunguzi wa kisasa umeonyesha kwamba kila namna ya ndege wana njia zao za kufahamiana wao kwa wao. Katika njia hizo ni kwa kugusa, na sauti, na ishara.

27:18 - “Mpaka walipo fika kwenye bonde la wadudu chungu, alisema mdudu chungu mmoja: Enyi wadudu chungu! Ingieni majumbani mwenu, asikupondeni Sulaiman na majeshi yake bila ya wao kutambua.” Inafahamikana wazi katika Aya hii kuwa wadudu chungu wanaishi kwa makundi, yaani wana umoja, na moja katika sifa zao ni kuwa macho na kutahadhari. Na inajulikana tangu zamani kuwa wadudu chungu wana sifa kadhaa wa kadhaa makhsusi ambazo zinaonyesha kuwa wana umoja wenye nidhamu madhubuti katika hukumu, na wana kiasi kikubwa cha akili, na werevu, na nguvu za kukumbuka, na kupenda kazi na kukakamia, na juhudi isiyo jua kunyong’onyea wala kukata tamaa. Kama wanavyo juulikana kuwa wana wingi wa hila za kuendesha kazi zao. Na dalili ya hayo ni kuwa jamaa wa wadudu chungu ni pekee yao baada ya binaadamu ndio wanao zika maiti wao. Na makundi mbali mbali yao yanashughulikia kukutana pahala pamoja kwa nyakati maalumu. Kwa ajili ya hayo zimewekwa siku makhsusi za kusimamisha soko wanapo kusanyika makundi yote kwa kubadilishana bidhaa na kujuana. Na makundi haya yanapo kutana hutokea mazungumzo kwa hima kubwa, na huulizana masuala yaliyo khusiana na mambo yao. Katika yanayo onekana yaliyo fungamana na mikusanyiko hiyo ni kuzuka mashauri yaliyo khusu umma wao, kama kutengeneza barabara ndefu, kwa subira na kukakamia kunako staajibisha. Wala makundi haya hayatosheki na kufanya kazi mchana tu, bali huendeleza kazi zao katika masiku ya mbaamwezi; ama masiku ya kiza hubaki mwahala mwao. Na jamaa wa makundi haya wana njia za pekee za kukusanya na kubeba na kuhifadhi vifaa vyao vya kula. Akishindwa mdudu kuchukua chakula alichokwa kwa mdomo wake hukisukuma kwa miguu yake ya nyuma, na akakinyanyua kwa mikono yake. Na katika mtindo wao ni kuzing’ong’ona mbegu, na kuzipasua baadhi ya nafaka kabla ya kuzirindika ili zisije kuchipua. Na mbegu kubwa kubwa huzigawa vipande vipande ili iwe wepesi kuziingiza katika ghala zao. Na pindi zikiroana kwa mvua huzitoa zipate upepo na jua zikauke.

27:22 - “Basi hakukaa mbali, na akasema: Nimegundua usilo gundua wewe, na ninakujia hivi kutoka nchi ya Sabai, na nakuletea khabari za yakini. Hakika mimi

nimemkuta mwanamke anawatawala, naye amepewa kila kitu, na anacho kiti cha enzi kikubwa. Nimemkuta yeye na watu wake wanalisujudia jua badala ya Mwenyezi Mungu; na Shetani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia Njia. Kwa hivyo hawakuongoka.” Hizi ndizo Aya khasa zilizo khusu Ufalme wa Sabai. Na hii Sabai ni moja katika falme za kusini ya Arabuni, inayo itwa Yaman, na ambayo zamani ilikuwa ni maarufu kwa jina la “Arabia Iliyo Neemeka”. Na jina hili la mwisho linaonyesha maendeleo yake na utajiri wake. Kwani kwa hakika ilikuwa nchi hiyo ina ustaarabu wa juu tangu miaka elfu mbili kabla ya kuzaliwa Nabii Isa a.s. Ikitegemea makulima, kwa sababu ya rutuba ya ardhi yake, na uzuri wa hali yake ya hewa. Na pia ikitegemea biashara kwa kuwa ipo kati baina ya Bara Hindi, na Uhabeshi, na Somalia, na Sham, na Iraq. Na kwa hakika mahodhi yaliyo jengwa kuwekea maji na kuyatumia, na maarufu yao yote ni Hodhi Maa’rib (Tazama Aya 16 Surat Sabai) na miji iliyo jengewa ngome, na makasri, na mahekalu, yanashuhudia mpaka hii leo maendeleo ya kijamii ya utajiri ulio kuwako katika nchi hii.

Na hakika nakshi walizo zinakishi watawala wao, na baina ya nakshi hizo zipo kanuni za kuendesha mambo ya ujenzi na mengineyo, yanaonyesha kwa kila dalili ukomo wa ustaarabu ulio nawiri walio ufikilia. Na huu ufalme wa Sabai ambao ulifikilia kilele cha kustawi kwake katika siku za Sulaiman a.s. kiasi ya karne kumi kabla ya kuzaliwa Nabii Isa a.s. ulikuwa ni ufalme kama wa kabla yake, yaani watoto wakiwarithi baba zao. Na kwa hivyo alikuwa akihukumu wakati wa Sulaiman a.s. Malkia. Wataalamu wa taarikh wamekhitafiana juu ya jina la Malkia huyo. Waarabu wakimwita Balqis; akisaidiwa na wazee wahishimiwa kama ni Baraza la Mashauri lake. (Tazama Aya 28-33 katika Surat An-naml.) Wala haikuthibitisha taarikh (historia) kuwa Ufalme wa Sabai ulikuwa dola ya kuteka nchi, bali ulikuwa ufalme wa biashara, na misafara. Katika mabaki yake hatuoni kutajwa vita au kuteka nchi isipo kuwa kwa uchache. Na haya ni kuwa umuhimu wa majeshi yake ulikuwa ni kuhifadhi ngome zake na kuzihami, na kulinda misafara yake kwa aghlabu. Na wananchi wa Sabai walikuwa ni mapagani, makafiri, wakiliabudu jua, kama ilivyo kuja katika Aya tukufu nambari 24 katika Sura hii. Pia wakiabudu mwezi. Na hao ndio miungu yao muhimu kabisa. Na walikuwa wakiwatolea sadaka na wakifukiza ubani katika mahekalu yao.

27:82 - Hii ndio tafsiri ya Aya hii kwa dhaahiri ya matamko yake. Na zipo tafsiri mbili nyengine ambazo za hii Aya zinazo weza kuwa: Kwanza ni kuwa makusudio ya “*Dabbah*” ni yeyote aendaye “yadibbu”, katika watu au wengineo. Na hapa inachukuliwa kuwa ni watu, watao kuja kabla ya Kiyama. Na maana yake ni kuwa ikiwateremkia kauli juu yao na adhabu ikathibiti watakuja makundi ya Waumini wakiwaendea, wakienea kote kote, wakizitikisa nguzo za ukafiri. Tafsiri ya pili neno hilo “*Dabbah*” makusudio yake ni watu waovu, ambao kwa ujinga ni kama wanyama, kama alivyo sema Al As’fahan katika Muqarrarat yake. Na maana yake ni kuwa ikikaribia Siku ya Kiyama, uovu na ufisadi utazidi, na Kiyama wanacho kikanusha makafiri ndio kitakuja. Na hiyo kauli itakuwa, nayo si kauli ya kutamkwa kwa mdomo, lakini kwa kuwa hali yenyewe itakuwa hivyo ni kama iliyo semwa, kama maoni yaliyo kwisha tangulia.

27:88 - “Na unaiona milima unaidhunja imetulia; nayo inakwenda kama mwendo

wa mawingu. Huo ndio ufundi wa Mwenyezi Mungu aliye tengeneza vilivyo kila kitu. Hakika Yeye anazo khabari za yote myatendayo.” Aya hii inathibitisha kuwa vitu vyote vinavyo fuata mvutano wa ardhi, kama milima, bahari, na funiko la anga n.k. vinashirikiana na dunia katika mzunguko wake wa kila siku juu ya msumari-kati wake, na mzunguko wake wa kila mwaka kulizunguka jua. Lakini mzunguko huu hauonekani. Ni kama kwenda kwa mawingu angani. Wanao tazama wanayaona, lakini hawasikii sauti yao, wala hawayagusi. Inaonyesha Aya hii tukufu kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu aliye tukuka, ameumba ulimwengu na mipango yake ya kuiendeshea. Naye ni Muweza wa kuifanya hii dunia imetulia tu haizunguki juu ya msumari-kati wake, au akaifanya kuzunguka juu ya msumari-kati wake sawa sawa na kuzunguka kwake kulizunguka jua. Na kwa hivyo ingeli kuwa nusu ya dunia imo kizani totoro kwa muda wa miezi sita, na kwa muda wa miezi sita ikawa nusu ya pili imo katika mwangaza moja kwa moja wa mchana. Na haya yangeli pelekea kuharibika mizani ya joto katika dunia yote. Na kwa hivyo uhai ulioko ungeli toweka duniani. Na Mwenyezi Mungu, Subhanahu wa Taa’la, ndiye aliye panga mpango huu uliopo kwa rehema yake na huruma zake kwa waja wake. Na juu ya kuwa Aristakhoris, mtaalamu wa ilimu ya falaki wa Iskandaria (Alexandria) katika Misri, aliandika (310-230 K.K.) juu ya kuzunguka dunia wenyewe kwa wenyewe, maandishi haya ya kisayansi ya kale yalikuwa hayajawafikia Waarabu wakati wa Mtume Muhammad s.a.w. au kabla yake. Bali wa mwanzo wa kuashiria mambo haya katika wao alikuwa Albiruni katika mwaka 1000 B.K. (Baada ya Kuzaliwa Nabii Isa), baada ya kuingia kufasiriwa vitabu vya ilimu za zamani kwa lugha ya Kiarabu ulio kuweko katika enzi za Banul Abbas. Basi kutokea haya kwa ulimi wa Mtume Muhammad s.a.w. ambaye aliye kuwa hajapata ilimu hiyo, ni dalili kuwa haya yalifunuliwa kwake na Mwenyezi Mungu.

28:73 - “Sema: Mwaonaje, Mwenyezi Mungu angeli ufanya usiku umekukalieni moja kwa moja, mungu gani asiye kuwa Mwenyezi Mungu atakaye kuleteeni mwangaza? Basi je, hamsikii? Sema: Mwaonaje, Mwenyezi Mungu angeli ufanya mchana umekukalieni moja kwa moja mpaka Siku ya Kiyama, mungu gani asiye kuwa Mwenyezi Mungu ataye kuleteeni usiku mkapumzika humo? Basi je, hamwoni? Na ni katika rehema zake amekufanyieni usiku na mchana mpate kupumzika humo na mtafute fadhila zake, na ili mpate kushukuru.” Hapana shaka kuwa kuumbwa kwa dunia kwa namna yake ilivyo sasa na ilivyo wekwa kwa mnasaba wa jua, na kuzunguka kwake wenyewe kwa wenyewe kila siku, na kulizunguka jua kila mwaka, hapana shaka kwamba haya yanaonyesha dhaahiri uwezo wa Mwenyezi Mungu na upweke wake.

Na Aya tukufu inawazindua watu watambue ukweli ambao yawapasa waelewe, nao ni kwamba Yeye Mtukufu lau kuwa aliumba dunia iwe na usiku wa milele, au iwe na mchana wa milele, basi hapanapo mungu mwengine anaye weza kuwaneemesha watu kwa mchana na usiku wa kufuatana kama hivi.

Na hivyo ni kuwa lau kuwa dunia inazunguka juu ya msumari-kati wake na pia kulizunguka jua kwa kiwango kimoja kiasi ya siku 365 takriban, yangeli tokea mabadiliko makubwa mno. Miongoni mwao ni kudumu giza katika nusu ya dunia, na kudumu mwangaza katika nusu ya pili takriban. Na kwa hivi joto lingeli panda katika nusu yenye mwangaza kwa kiasi kisicho weza kuchukulika. Na nusu yenye

giza ingeganda kwa barafu. Na pande zote mbili zisingeweza kuchukua kitu chochote chenye uhai. Ama huu mpango ulivyo sasa unapelekea kupishana usiku na mchana, na kwa hivyo kunapatikana mapumziko na utulivu wakati wa usiku, na kushughulika wakati wa mchana. Na hali ya hewa inasiliki uhai wa binaadamu, na wanyama, na mimea. Na haya ni katika fadhila za Mwenyezi Mungu juu ya waja wake, ambazo zinapelekea tukubali uwezo wake, na tudumu kumshukuru.

29:20 - “Sema: Tembeeni katika ardhi na tazameni jinsi alivyo anzisha uumbaji; kisha Mwenyezi Mungu ndiye anaye umbu umbo la baadaye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.” Aya hii tukufu inawahimiza wachunguzi wende katika dunia wapate kuvumbua vipi ulianza uumbaji wa vitu, tangu wanyama, na mimea mpaka visio kuwa na uhai. Kwani mabaki ya uumbaji wa mwanzo yamehifadhiwa baina ya tabaka za ardhi na juu yake. Na kwa hivyo ardhi ni daftari lililo sajiliwa ndani yake taarikhii yote ya uumbaji, tangu mwanzo wake mpaka hivi sasa.

29:41 - “Mfano wa walio wafanya walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, ni mfano wa buibui alivyo jitandia nyumba. Na hakika nyumba dhaifu mno kuliko zote ni jumba la buibui, laiti kuwa wanajua.”:

Nyumba za buibui anazo jenga kwa ajili ya maskani yake na kwa ajili ya kukamatia mateka wake zimeundwa kwa wembamba mno, kwani hizo ni nyuzi zilizo kuwa hadi ya mwisho wa wembamba, zinashinda wembamba wa hariri. Na kwa hivyo mfumo wake umekuwa ni wa mwisho wa udhaifu kuliko nyumba zote walizo jijengea wanyama kuwa ni makaazi yao.

30:4 - Maoni ya wataalamu juu ya Aya 1- 4:

Katika Aya hizi tukufu ipo ishara ya vituko viwili. Cha kwanza kilikwisha tokea khasa. Na cha pili kilikuwa bado hakijatokea, na hayo ni kutoa khabari ya ghaibu. (Na imetajwa kuwa yatatokea mnamo miaka michache, ambayo maana yake ni mitatu mpaka tisa.)

Na maelezo ya tukio la mwanzo ni kuwa Waajemi na Warumi walipambana kwa vita katika nchi ya Shamu katika enzi za Khasro Abrawiz, au Khasro wa Pili, Mfalme wa Uajemi, maarufu kwa Waarabu kwa jina la Kisra, na Heraklius Mdogo, Mfalme wa Wafalme wa Kirumi, ambaye kwa Waarabu ni maarufu kwa jina la Heraklu. Katika mwaka 614 Uajemi iliiteka Antiokia, mji mkubwa kabisa katika jimbo la Mashariki katika Ufalme wa Rumi, na baadae ikatekwa Dimishqi (Damask), na ukazingwa mji wa Baitul Muqaddas (Yerusalemu) mpaka ukasalimu amri. Wakauunguza, wakawaingilia wakaazi wake kuwachinja. Moto huo uliteketeza Kanisa la Kiyama. Wavamizi hao waliuchukua Msalaba wakaupeleka kwenye jiji lao. Nyoyo za Wakristo zilihuzunika sana kwa msiba huu wa kutisha. Ilivyo kuwa kushindwa huku kuliwaleteta furaha washirikina wa Makka na wakawa wanawafanyia tashtiti Waislamu kwa kuwa Warumi ni Watu wa Kitabu kama watu wa Muhammad s.a.w., na Waajemi kama washirikina si Watu wa Kitabu, basi Mwenyezi Mungu Mtukufu aliye tukuka alimteremshia Muhammad Aya hizi zilizo wazi ili ambashirie kuwa Watu wa Kitabu watakuja shinda, nao Waumini watafurahi. Na kushindwa kwa washirikina na uovu wa khatima yao kuliwekewa kiwango cha miaka michache.

Na ufafanuzi wa tukio la pili ni kuwa Heraklu, Kaisari wa Rumi, ambaye jeshi lake lilishindwa, hakukata tamaa kuwa atashinda. Akawa anajiandaa kwa ajili ya mpambano utakao futa ari ya kushindwa. Mpaka mwaka wa 622 wa kuzaliwa Nabii Isa a.s., yaani mwaka wa kwanza wa Hijra Waajemi wakalazimika kuingia vita katika nchi ya Arminia. Huko Warumi wakashinda. Na ikawa hapo ndio chanzo cha ushindi mara nyingi wa Rumi kuishinda Uajemi. Ndio hivi Watu wa Kitabu wakawashinda washirikina, na ukweli wa bishara ya Qur’ani ukathibiti.

Na tena kituko cha tatu kinafahamika kwa maana kutokana na Aya hizi tukufu, nacho kikaleta furaha kwa Waislamu. Nacho ni kushinda kwao kuwashinda washirikina Makureshi katika Vita vya Badri vilivyo tokea siku ya Ijumaa, 17 Ramadhani mwaka wa pili wa Hijra, yaani mwaka 623 wa kuzaliwa Nabii Isa a.s.

31:13 - Waarabu walikuwa wanawajua watu wawili kwa jina hili. Mmoja wapo ni Luqman bin A’adi. Nao walikuwa wakimtukuza cheo kwa werevu wake, uraisi, ujuzi, ufasihi na ujanja. Na walikithiri sana kumtaja na kumpigia mithali, kama inavyo onekana katika vitabu vya Kiarabu vingi. Ama mwengine ni huyo anaye itwa Luqman Alhakim, (Mwenye hikima), aliye kuwa mashhuri kwa hikima yake na mifano yake, na ambaye Sura hii ya Qur’ani imeitwa kwa jina lake. Na hikima zake zilikuwa zimeenea kwa Waarabu. Ibn Hisham amesimulia kwamba Suwaid bin Ass’amit alifika Makka. Naye alikuwa mtu mtukufu kwa watu wake. Mtume s.a.w. akamtaka asilimu. Suwaid akasema: Huenda labda uliyo nayo wewe ndiyo kama niliyo nayo mimi. Mtume s.a.w. akasema: Nini ulicho nacho? Akasema: Majalla ya Luqman. Mtume s.a.w. akasema: Nisomee. Akamsomea. Tena akasema: Hakika haya maneno mazuri. Na niliyo nayo mimi ni bora zaidi, nayo ni Qur’ani aliyo niteremshia Mwenyezi Mungu, nayo ni Uwongofu na Nuru. Mtume s.a.w. akamsomea Qur’ani na akamtaka asilimu. Na pia Imam Malik ametaja kwa wingi hikima za Luqman katika kitabu chake, Al Muwatt’a. Na baadhi ya vitabu vya Tafsiri ya Qur’ani na Adab (maandishi ya ufasihi wa lugha) vimetaja namna mbali mbali katika hikima hizo. Kisha baadae ikakusanywa mithali kwa visa katika kitabu chenye jina la Mithali za Luqman. Lakini kwa sababu ya udhaifu wa mpango wake, na wingi wa makosa ya nahau na sarfu, na kuwa kutopokewa kitabu cha jina hili katika vitabu vya Waarabu wa kale, yatilia nguvu kuwa hichi kimezuliwa tu katika zama za mwisho. Na maoni yanayo gongana juu ya uhakika wa Luqman Alhakim: ni kuwa yeye ni Mnubi katika watu wa Abla au Uhabeshi, au mtu mweusi wa Sudan ya Misri, au ni Muibrani. Na wengi walio mtaja wanakubaliana kuwa hakuwa Nabii. Wachache tu ndio wanasema kuwa alikuwa Nabii. Na tunalo weza kutambua katika yaliyo tajwa ni kuwa hakuwa Mwaarabu, kwa sababu wote wamewafikiana kwa hayo. Na kwamba alikuwa ni mtu mwenye hikima, na hakuwa Nabii, na kwamba ameingiza miongoni mwa Waarabu hikima mpya zikawa zinatajwa mara nyingi kama ilivyo onekana baadae katika vitabu.

32:8 - Katika Aya hii tukufu “utokane na kizazi cha maji dhaifu”. Neno la Kiarabu lilio tumiwa ni “Mahiin”. Neno hili likitumiwa kwa mtu lina maana ya “dhaif”, mnyonge, na pia lina maana ya “chache”. Basi kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Min maain mahiin” maana yake ni “kutokana na maji machache dhaifu”, ndiyo ya kudharauliwa. Mfano wa hayo ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Au mimi si bora kuliko

huyu aliye (mahiin) mnyonge wala hawezi kusema waziwazi?” (Azzukhruf: 43:52). Na neno “Mahana al-ibila” maana yake “Kamkama maziwa ngamia”. Kwa hivyo basi hapana ubaya kulifasiri neno hili Mahiin katika Aya hii kwa maana ya maji yanayo toka kwa kuchupa, au kumiminika, (kama yanavyo toka maziwa kwenye chuchu) au machache.

33:10 - Si makusudio ya maneno haya kuwa maadui walikuja kutoka kila upande. Tukiangalia ufafanuzi wa tukio hili inadhihirika kuwa makusudio ni kuwa walio kuja kutoka upande wa juu ya Waislamu, ni kabila ya Ghat’fan na walio wafuata katika wakaazi wa Najdi, kwani wao walikuja pande za juu ya Bara Arabu upande wa mashariki. Na inatudhihirikia kuwa walio kuja upande wa chini ya Waumini ni Makureshi, kwa sababu wao walikuja kutoka upande wa chini ya Bara Arabu upande wa magharibi.

33:19 - Aya hii tukufu inaashiria ukweli wa kisayansi ambao ulikuwa haukujuulikana namna yake wakati wa kuteremka Qur’ani Tukufu. Ukweli huo ni kuwa jicho wakati wa kukurubia mauti au wakati wa khofu huzunguka. Na katika sababu za hayo ni kuwa kwa shida ya khofu utambuzi hutoweka, ikawa mtu hajitambui. Vituo vya navo zisio tambua katika ubongo hupoteza mizani yake, basi huwa huyo mwenye khofu kama mfano wa mwenye kuzimia kwa kukaribia kufa, jicho lake huzunguka na mboni ya jicho hupanuka, na hubaki katika hali ya kukodoa macho mpaka kufa.

33:53 - Yanarejea maelezo ya ki-ilimu juu ya Aya mbili 58, na 59 za Surat An-nur, katika yaliyo khusu adabu za kuzuru.

34:3 - Dharra , tuliyo ifasiri “Chembe”, na kisayansi ni Atom kwa hakika katika lugha ya Kiarabu ni kitu kidogo sana, kama sisimizi mdogo, au chembe ya vumbi. Na uzito wa Dharra maana yake ni uzani wake. Na Aya inaonyesha kuwa kipo kilicho kuwa ni kidogo kuliko Dharra. Na yafaa kutaja hapa kuwa sayansi za sasa zimethibitisha kuwa Dharra, yaani Atom, imegawika katika sehemu ndogo zaidi nazo ni Nucleus na Electrons. Na haya hayakuthibitika ila katika karne ya ishirini ya kuzaliwa Nabii Isa.

34:10 - Daudi, a.s. ni mmoja wa Manabii wa Wana wa Israili, na mmoja wa wafalme wao. Aliishi katika zama za baina ya mwaka 1010 na 970 K.K. (yaani kabla ya kuzaliwa Nabii Isa a.s.)

34:16 - Hili liitwalo “Hodhi” la maji ya mvua kubwa au “Hodhi la Ma`arib” ni kubwa kuliko mahodhi yote ya Yaman. Hodhi hili linaweza kubadilisha ardhi kavu ya kiasi ya maili 300 ya mraba ikawa yenye rutba na mashamba. Na dalili ya hayo ni hizo bustani mbili zilizo tajwa. Wanazuoni wa taarikh (historia) wanakhitalifiana katika ujenzi wa hilo hodhi kuu. Vile vile zipo kauli mbali mbali kukhusu kubomoka kwake.

35:12 - Na katika Ishara za Mwenyezi Mungu ambazo anawaitia watu wazizingatie na ambazo amewaneemesha fadhila zake ni mwendo wa marikebu na kukata kwake maji baharini kwa mujibu wa kawaida zake alizo ziwekea katika tabia za maumbile,

nazo ni hizo sharia za vitu kuelea, (The law of buoyancy). Ni maarufu kuwa baadhi ya mapambo yanapatikana kutoka maji ya chumvi, na baadhi ya watu labda wanaona haiwi maji matamu kutoa mapambo vile vile. Lakini ilimu na mambo yalivyo yamethibitisha kinyume cha hivyo. Ama lulu kama zinavyo patikana katika maji ya chumvi, basi vile vile zinapatikana kwenye namna fulani nyengine za chaza wa mitoni. Hupatikana lulu katika maji matamu katika Uingereza, Scotland, Wales. Czechoslovakia na Japan.. n.k. mbali na lulu za baharini maarufu. Na pia vinaingia katika vinavyo patikana katika maji matamu maadini thamini ngumu kama almasi, zinazo patikana katika udongo unao tupwa na mito. Hupatikana pia Yaakuti, katika mito ya Mojok karibu na Andalas katika Burma ya juu. Ama katika Siam (Thailand) na Sri Lanka hupatikana Yaakuti katika mito. Na katika mawe ambayo yashabihiana na ya ghali na hutumiwa kwa pambo ni Topaz. Na hupatikana pia kwenye mito mwahali mwingi katika Brazil na Urusi (Ural na Siberia) Fluro-sylicate of aluminium. Aghlabu hiyo huwa ya manjano au rangi ya kahawia. Circom ni jiwe thamini linavutia. Sifa zake zinakaribia za Almasi. Namna zake nyingi hupatikana kwenye mito. (Kadhaalika dhahabu, ambayo inaitwa Alluvial gold yaani dhahabu ya mtoni, hupatikana nchi nyingi, mojawapo ni Zaire.)

35:13 - Aya hii tukufu inaonyesha kuwa jua lina muda utakao kwisha baadae. Na huenda kuwa huo ndio utao kuwa Mwisho kwa mujibu wasemavyo wataalamu wa ilimu ya Falaki (Astronomy) kwamba jua linaunguza kuni zake za Dharra (Nuclear fuel) nayo ni Hydrogen inayo geuka kuwa Helium. Huenda kuwa ukisha muda wa jua ndio Msiba Mkuu wa Ulimwengu wote.

35:27 - Ya kustaajabisha kitaalamu katika Aya hii tukufu sio tu kwa kukhitalifiana rangi mbali mbali katika milima, ambazo zinatokana na hizo sehemu za maadini zilizo fanya majabali, kama vile chuma huonyesha rangi yake nyekundu, na manganese na makaa ya mawe huonekana kwa rangi nyeusi, au shaba ambayo hudhihirisha rangi ya kijani n.k. Lakini ya kustaajabisha khasa ni kuunganisha baina ya kutoa matunda ya namna mbali mbali na hali miti yake inanyweshwa maji yale yale, na kuumbwa milima myekundu, na myeupe, na nyeusi, na yote yana asli moja kwa kuundwa kwake. Wataalamu wa ilimu za t'abaka za ardhi, Jiolojia, wanaita Magma. Na hii Magma moja inapo chomoza pahala mbali mbali katika ardhi, na penye vina mbali mbali (kwenda chini) katika ardhi kutoka juu basi hupatikana khitalafu katika muundo wake na hukusanyika kwa kurindika kuwa ni milima yenye maadini ya rangi mbali mbali. Na huu basi mwendo wa Mwenyezi Mungu ni mmoja. Kwani hakika asli ni moja, na matawi ndiyo yanakhitalifiana kwa kuonekana. Na katika haya yanapatikana manufaa na faida kwa binaadamu.

35:28 - Baada ya kueleza kukhitalifiana matunda, na milima, na watu, na wanyama, na mifugo, inaashiriwa kuwa juu ya khitalafu hizi zinazo onekana baina ya hali hizi zote, upo umoja wa asli. Kwani hayo matunda yanatokana na maji yale yale. Na milima inatokana na Magma moja. Kadhaalika khitalafu za rangi, na watu, na wanyama, na mifugo, hazidhihiri katika tone za manii ambavyo vyote hivyo vimetoka mwanzo wake. Na lau hizo tone zingeli chunguzwa kwa darubini ya Maikroskopu kisingeli onekana kitu cha kuonyesha hizo khitalafu zitazo kuwa. Kwani hizo ni siri zilioko

ndani yake katika zinazo itwa Genes (Jiinz). Na labda haya pia yanaonyesha kuwa sifa za kurithi ziliomo katika asli ya mimea, na wanyama, na binaadamu, zinalindwa katika maumbile yake, na hazigeuki kwa tabia ya pahala au chakula.

35:41 - Aya hii tukufu inathibitisha kwamba Mwenyezi Mungu Subhanahu wa Taa'la peke yake ndiye Muumba mbingu na ardhi. Yeye ndiye Mwenye kuzishika zisiondoke. Kwani hivi vitu viliomo mbinguni vya karibu na mbali vinavyo onekana katika qubba la mbingu vimeshikamana kwa mujibu wa mpango maalumu wa namna ya pekee alio uumba Mwenyezi Mungu Aliye takasika na Kutukuka. Na Yeye ndiye aliye viwekea mvutano usio katika kwa kupita zama na vizazi, na ndiye anaye vihifadhi visikosee mizani yao. Na Mwenyezi Mungu Subhanahu wa Taala ndiye Mwenye uweza huu, wala hapana mwenginewe.

36:13 - Baadhi wa wafasiri wanasema mji huo ni Antiokia.

36:36 - Hii harufi Min , yaani “Katika” katika Aya hii ni ya kubainisha. Maana yake Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba madume na majike katika viumbe vyake vyote, sawa sawa katika mimea, na wanyama, na wanaadamu na vyenginevyo ambavyo watu hawavijui na hawavioni.

36:40 - Hakika Aya hizi tukufu zinabainisha ukweli wa ki-ilmu ambao wataalamu walikuwa hawaujui ila mwanzo wa karne ya kumi na nne ya kuzaliwa Nabii Isa. Na jua ni moja katika nyota za mbinguni, nalo kama nyota zilizo baki lina mwendo wake wenyewe. Lakini linakhitalifiana na nyota nyengine kwa kuwa lipo karibu na dunia, na kwa kuwa lina kundi la sayari na miezi ya mikia na sayari ndogo ndogo zinazo lifuata daima, na zinat'ii mvuto wake. Kwa hivyo zinakuwa hizo zinazunguka kwa kufuatana kwa utungo kama sura ya yai. Na mkusanyo wote huu unakwenda angani pamoja na jua kwa mvuto wake. Kwa ufupi jua, na ardhi, na mwezi na sayari zote na vyombo vyote hivyo vinakwenda angani kwa mbio maalumu, na kuelekea jiha maalumu. Na yaonekana kuwa jua na mkusanyo wote huo wake, na nyota zilizo karibu nalo zipo katika mkusanyo ulio tanda katika mbingu inayo itwa kwa Kiarabu Sadiimu almajarra, au kwa Kiingereza Nebula course. Na imebainika kwa masomo ya kisasa sehemu zote za hiyo Nebula zinaizunguka kati yake kwa mbio ya kunasibiana na kinyume cha umbali wake kutoka hapo kati. Pia imeonakana kuwa jua na ardhi na sayari zake na nyota zilizo karibu nayo, vyote hivyo vinakwenda mbio, na upande maalumu. Mbio zake zinafika kilomita 700 kila nukta moja. Na kunatimia kuzunguka kwake kukizunguka hicho kituo cha kati kwa kiasi ya miaka milioni 200 ya muangaza. Na kiini cha maneno ni kuwa Aya tukufu iliyo taja kuwa jua linakwenda kwa kiwango chake, hawakujua wataalamu uzuri wake wa ndani mpaka katika mwanzo wa karne hii (ya ishirini). Wala hayamkini jua kuupata mwezi, kwani kila kimojapo kinakwenda katika njia zake mbali mbali, basi ni muhali kukutana, kama ilivyo kuwa ni muhali kupitana usiku na mchana. Hayo ingeli takikana ardhi izunguke juu ya msumari-kati wake kutoka mashariki kwendea magharibi, kinyume na ilivyo hivi sasa kutoka magharibi kwendea mashariki. Na mwezi katika kuizunguka kwake ardhi, na ardhi kulizunguka jua, huenda pamoja na mkusanyo wa nyota unao itwa Manaazil Alqamar

au Lunar system. Na katika robo ya mwanzo na ya mwisho wa mwezi huonekana sura yake kama karara kongwe au kole lilio kauka, linapo kuwa kongwe na kunyauka.

36:68 - Na tunaye mfanyia umri wake uwe mrefu tunamrejesha awe kinyume na alivyo kuwa. Yaani baada ya kuwa na nguvu anakuwa dhaifu. Hayo ni kwa kuwa maisha ya mwanaadamu yanapitia vipindi vitatu, kukua, kutimia kukua; na ukongwe unaanza kwa kunywea kwa mafigo, ini, Ghudda Ddarqiya au Thyroid gland, na Pancreas, yaani Dongoronya. Na haya huleta athari katika kudhoofika mwili wote. Mishipa ya damu nayo huanza kukacha na kunywea, na kwa hivyo hupunguka damu inayo kwenda katika viungo vyote vya mwili, basi ndio huzidi udhaifu juu ya udhaifu. Na katika sababu za kukonga ni kuzidi nguvu za kubomoka kuliko kujengeka katika mwili, yaani Metabolism. Na hayo ni kwa kuwa Khalaya au Cells, za mwili zote zimo katika hali ya kugeuka, na pia Khalaya za damu, isipo kuwa Khalaya za ubongo wa kichwani na wa katika mifupa. Hizo hazigeuki muda wote wa uhai. Ikiwa kiasi ya kuundika upya ni sawa ya kiasi cha kuharibika, basi hapana madhara yanayo tokea. Lakini ikiwa kuharibika ni kukubwa kuliko kujengeka katika kiungo chochote basi hapo hudhihiri madhara kwenye kiungo hicho. Na kwa hivyo kila umri ukiwa mkubwa kiasi cha kujengeka kinapungua na kinazidi kiasi cha kubomoka kwa Khalaya, na kunadhihiri kunywea, na kupungua nguvu kote. Na hukhitalifiana kiasi cha kujengeka kwa mnasaba wa kubomoka kwa kukhitalifiana namna ya mfumo (Nasij, Texture). Katika hayo yanayo dhihiri kama ngozi iliyo funika mwili, na zililo funika paipu za kusaga chakula, na paipu za Ghudad, Glands, zinachakaa kwa upesi zaidi kila miaka ya binaadamu ikipita. Na hii ni sababu ya kuonekana upesi alama za kuzeeka.

36:80 - Nguvu za jua zinaingia ndani ya mimea kwa wasita wa mwangaza. Khalaya zenye madda ya kijani katika mimea Chlorophyl ndizo zinafyonza Carbon dioxide kutokana na hewa, na hii huchanganyika na maji yanayo fonzwa na mimea, na kufanyika Carbohydrates kwa kuathiriwa na nguvu zinazo tokana na mwangaza wa jua. Tena hufanyika mbao, kuni, ambazo sehemu kubwa ni muundo wa kimyaa wa Carbon na Hydrogen na Oxygen. Na kutokana na kuni hizi hufanyika makaa haya ya miti tuyatumaiyo. Ukiyachoma makaa hutoka nguvu zilizo kuwamo ndani yake kwa ajili ya kupikia, na kwa kazi nyingi nyenginezo. Na makaa ya mawe si chochote ila ni hiyo hiyo mimea na miti iliyo kuwa na kufanyika kama ilivyo elezwa, na kisha ikazikika kwa njia fulani na kugeuka baada ya kupita mamilioni ya miaka kuwa makaa ya mawe, kwa kuathirika na hali za geology kama joto au mdidimizo au mengine. Na yapasa kuzingatia kuwa kutajwa katika Aya hii “mti wa kijani” si bure, bali ni ishara ya hiyo Chlorophyll ya kijani ambayo ni lazima kwa ajili ya kuimeza Carbon dioxide katika mimea.

37:5 - Mwenyezi Mungu ndiye Muumba mbingu saba na viliomo baina yao, navyo ni hivyo vyombo vya mbinguni na nyota zake. Naye ndiye Mwenye kusimamisha, Mwenye kulinda vile vile juu ya mwahali zinapo chomozea jua na nyota zote. Na Yeye ndiye anaye vionyesha hivyo kila siku katika pahala huko upeo wa macho, kila siku pahala mbali na vilipo dhihiri siku iliyo tangulia. Na hayo ni kwa mwendo wa mpango wa jua maalumu kwa inavyo zunguka dunia juu ya msumari-kati wake

kutoka magharibi kwendea mashariki kila siku na wakati huo huo inavyo lizunguka jua katika njia yake katika falaki. Na jua na nyota huonekana na wakaazi wa ardhi kila siku kama zinachomoza mwahala mbali mbali. Na kila ardhi ikigeuza mahala pake katika safari yake katika mbingu linaonekana jua linachomoza pahala pengine. Ukiliangalia jua kwa utulivu kuanzia mwishoni wa mwezi wa Machi, yaani linapo kuwa jua lipo kati ya mstari wa Ikweta mwanzo wa musimu wa Rabii, yaani Spring, kwa nusu ya kaskazini ya dunia, utalionga linachomoza pahala katika mashariki juu ya upeo wa macho. Kwa mwenye kupeleleza kila siku ikipita ataona kuchomoza kwake kunajongelea kaskazini. Na mwishoni mwa mwezi wa Juni utaona linachomozea mwisho wa kukaribia kaskazini. Kisha baada ya hapo utalionga jua linarejea linafuata kugeuka kule kule mpaka mwisho wa Septemba (wakati wa kuwa sawa wakati wa Khariif yaani Autumn) utalionga jua linachomoza pale pale lilipo chomoza mwanzo wa Machi. Kisha litaendelea kuelekea kusini kuchomoza kwake mpaka mwisho wa Desemba linakuwa linachomoza karibu kabisa na kusini. Baada ya hapo huanza tena kurejea kuelekea kaskazini mpaka limalize safari yake ya kufika kati sawa katika Rabii ya pili. Na safari hii yote inachukua siku 365 na robo siku. Na inaonekana kuwa nyota nazo zinachomoza mwahala mbali mbali katika upeo wa macho inapo kuwa dunia imo katika safari yake ya mbinguni, na khasa nyota za buruji (au vituo) 12 vinavyo pitiwa na jua katika mwendo wake wa mwaka.

37:145 - Yaliyo mtokea Sayyidna Yunus a.s. ni muujiza. Lakini nayo si muhali kutokea mtu kumezwa na samaki, na akabakia yuhai ndani yake kwa muda fulani. Mawili yaweza kuwa –

Kwanza, ni kuwa huyo samaki ni namna asiye kuwa na meno katika kabila ya nyangumi wakubwa kabisa, kama nyangumi wanao onekana sana katika Bahari ya Kati (Mediterranean). Urefu wake huweza kufika Mita 20. Alibaki Yunus katika mpandikizi wa kinywa chake huyo nyangumi mpaka alipo mtema kwenye ufukwe mtupu, kwani koo ya nyangumi ni nyembamba hawezi kupita mtu.

Pili, yaweza kuwa huyo samaki ni namna ya wenye meno pia, kama nyangumi wa ambari, na ambaye pia urefu wake hufika mita 20. Hawa mara kadhaa wa kadhaa huonekana katika Bahari ya Kati. Nyangumi hao yawezekana kwa kawaida kuwameza wanyama wakubwa wanao pita urefu wa mita tatu.

39:5 - Aya hii tukufu inaonyesha kuwa ardhi ina sura ya mvingo kama mpira, na inazunguka wenyewe kwa wenyewe juu ya msumari-kati wake. Kwani kule kutumiwa neno *Yukawwiru* katika Kiarabu na ikafasiriwa Hufunika, maana yake ni kufunika kitu kwa kitu kwa namna ya kufuatana, kukariri, mara kwa mara. Na lau kuwa ardhi haina sura ya mpira, kwa mfano kuwa batabata tu, usiku ungeli enea kote kwa ghafla, au mchana ungeli angaza dunia nzima kwa mara moja.

39:6 - Huzuka yai katika mwahala pa kufanyika mayai kwa mwanamke, hata likisha kuwa tayari hutumbukia katika mojapo ya paipu za Filopia likapita humo mpaka kufikia kwenye tumbo la uzazi Rahimi (Womb). Halifiki huko ila kupita siku kidogo, na huenda kijidudu cha manii (Sperm) ya mwanamume kikaliingia hilo yai, na hapo

huanza viwango vya kugeuka na kukua kwa mwanzo. Na katika tumbo la uzazi hubaki mtoto muda wa mimba, na hujifanyia vifuniko viwili, na sehemu ya funiko moja hufanyika zalio, placenta. Na funiko jingine ndio humfunika yule mtoto khasa.

Yapo maoni mbali mbali juu ya hivyo “viza vitatu” kama ilivyo tajwa katika Aya hii tukufu. Katika hayo ni

(1) Tumbo, na tumbo la uzazi, na zalio, yaani mfuko unao mfunika mtoto.

(2) Tumbo la uzazi, na ile mifuniko miwili.

(3) Tumbo na mgongo na tumbo la uzazi.

(4) Panapo toka mayai (Mabiidh, au Ovaries), na paipu ya kupitia mayai, Filloplan tube, na tumbo la uzazi (Rahimi au Womb).

Na dhaahiri ni kuwa hii ya mwisho ndiyo rai yenye nguvu zaidi, kwa sababu ni mahala patatu mbali mbali. Ama zile rai nyengine zinaonyesha kwa hakika kiza kimoja katika pahala pamoja palipo zungukwa na t’abaka kadhaa. Na Muumbaji Mtukufu ameashiria katika Kitabu chake ukweli huu wa kisayansi katika zama walipo kuwa watu hawajavumbua hayo mayai ya mwanamke na mwendo wake katika mwili ulio kuwa hauwezi kuonekana kwa macho.

39:7 - Haya yaliomo katika Qur’ani Tukufu yanaweka wazi msingi wa kutoa adhabu, kama ilivyo vile vile katika Surat Yusuf katika kauli yake Mtukufu: “Akasema: Mwenyezi Mungu apishe mbali sisi kumshika yeyote ila tuliye yakuta mali yetu kwake; hivyo basi tutakuwa madhaalimu.” Na haya katika Qur’ani ni kusimamisha msingi ulio kwisha tajwa, nao ni msingi ambao haukuthibiti katika kanuni (sharia) za kutungwa na binaadamu ila katika zama za karibuni. (Haya ni kinyume cha ilivyo katika imani aliyo itumbukiza Paulo katika Ukristo, kwamba wanaadamu wamerithi dhambi ya Adam, wanayo ita “Dhambi ya asili”, na kwamba Nabii Isa, Yesu, kafa msalabani kwa kubeba dhambi za wanaadamu. Biblia yenyewe inapinga haya. Tazama: Jeremiah 31:29-30; Ezekieli 18 Kwa nadhariya ya Paulo Mungu amedhulumu mara mbili:

1. Kutubandika wanaadamu wote dhambi za Adam,

2. Kumbebesha “mwanawe” Yesu dhambi za walimwengu wote!)

39:21 - Huku kuzunguka maji katika maumbile kutoka mbinguni na kufika kwenye ardhi na huko yakenda chini na kutimbuka katika chemchem, hakukuwa kunajuulikana kabla ya katikati za karne ya nane tangu kuzaliwa Nabii Isa a.s. Fikra iliyo zagaa kabla ya hapo ni kuwa maji ya chemchem na mito yanatimbuka kutoka chini ya ardhi kutoka kwenye mashimo na visima katika vina vya bahari.

39:63 - Injili ya Mathayo 16:16-20 imedai kuwa Yesu kampa funguo za mbingu na ardhi Petro, na hivyo ndiyo Papa wa Roma amerithi funguo hizo na kuanzisha Kanisa la Kikatoliki, na uwezo wa kufutia watu dhambi na kuwaangamiza Motoni. Marcello Craveri, mtaalamu wa Biblia wa Kitaliaana ameandika katika kitabu chake Maisha ya Yesu (sahifa 227-28 Panther Edn.) kuwa Mathayo 16:16-20 imeongezwa na ametoa hoja 7 kwa wazo hilo. Licha ya kuwa Yesu hakumpa Petro hizo funguo za mbingu na ardhi, yeye mwenyewe Yesu hakuwa nazo.

39:68 - Hilo barugumu (S’ur) kilugha, ni tarumbeta, mbiu, siwa, parapanda. Barugumu

inalo tusimulia Qur'ani ni katika mambo ya ulimwengu usio onekana, hatujui lilivyo na hakika yake.

40:11 - Na huenda yakaonyesha uhai wa Barzakh, ambao ni uhai makhsusi hatuujui hakika yake, aliyo yataja Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kauli yake juu ya watu wa Firauni: “Moto wanadhihirishiwa asubuhi na jioni; na siku itapo fika Saa ya Kiyama patanenwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa.” Na kauli yake Mtukufu: “Wala usiwadhania wale walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi.”

40:67 - “Yeye ndiye aliye kuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu..n.k.”

Maoni juu ya “Tone la manii”, “pande la damu” na “pande la nyama” yamo katika Aya 7,8 na 9 Sura Assajda; Aya 12, 13 na 14 Sura Al-Muuminuna; Aya 67 Sura Ghaafir; 5 Sura Al-Hajj. Neno Nut’fa katika lugha hutumika kwa maana ya manii ya mwanamume.

Tukirejea kwenye Aya Tukufu (75.37) “Je! Hakuwa tone la manii lilio shushiwa?” inadhihiri kuwa makusudi kwa “tone la manii” ni sehemu makhsusi ya manii. Na ilimu ya sayansi imevumbua kuwa makusudi ya sehemu hiyo ni kile kijidudu kinacho shushiwa, ambacho kinacho chukuliwa na maji yanayo shushwa, na kidudu hicho “Sperm” ambacho kikiingia kwenye kijiyai (Buwaydha Kiarabu au Ovum kwa Kizungu), cha mwanamke ndio huumbika mtoto.

Al-A’laqah katika maana zake kilugha ni damu iliyo ganda, au inayo tiririka iliyo nyekundu mno. Na ki-sayansi maana yake ni Khalaya, au Cells za Embryo (Mtoto ndani ya tumbo la mama) lilio gandamana (*ta-a’llaqa*) na ukuta wa tumbo la uzazi baada ya kwisha ingiana kidudu cha ume na yai la uke, na ikapatikana Khalaya moja ambayo ikagawika ikawa Khalaya kadhaa wa kadhaa zinazo endea kwenye ukuta wa tumbo la uzazi, kwenda kujibandika na huzua hapo kumwagika damu.

Al-mudhghah huyo ni mtoto katika mageuzi yake baada ya kutoka kuwa *Al-a’laqah*, yaani baada ya kwisha shikamana na ukuta wa tumbo la uzazi na kuviringana bila ya sura maalumu, na huzungukwa na vifuniko, na hubaki katika hali hiyo wiki chache hivi mpaka yafanyike mafupa. Na *Mudhghah* ambayo imefasiriwa kama pande la nyama ina khalaya zenye umbo maalumu, na hizo ndizo zinakuwa mtoto, na khalaya zisio kuwa na umbo maalumu, na hizi huzunguka sehemu ile iliyo timia umbo lake, na kazi yake ni kulinda na kutoa chakula.

Mafupa: Ilimu ya mimba Gynaecology imethibitisha karibuni kuwa mafupa yanadhihiri katika t’abaka ya katikati katika Khalaya za *Mudhghah* baada ya kutoka kiwango cha kugawanyika Khalaya za viungo.

41:9 - Zimetajwa Siku moja au Siku nyingi katika Sura nyengine. Katika Surat Al-Hajj, Aya 47 Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: “Na kwa hakika siku moja kwa Mola wako Mlezi ni kama miaka elfu mnavyo hisabu nyinyi.” Na katika Surat Assajdah, Aya 5 amesema Mtukufu: “Anapitisha mambo yote yaliyo baina ya mbingu na ardhi, kisha yanapanda kwake kwa siku moja tu ambayo kipimo chake ni miaka elfu mnayo hisabu.” Na katika Surat Al-Ma’arij Mtukufu amesema: “Malaika na Roho hupanda kwake katika siku iliyo kadiri yake ni miaka elfu khamsini.” Maoni

ya kitaalamu: Vipimo vya wakati wanavyo vitumia watu vimefungamana na dunia na inavyo zunguka juu ya msumari-kati wake na kulizunguka jua. Mtu akitoka kwenye ardhi (dunia) akenda kwenye sayari nyengine za mbinguni vipimo hivyo vya nyakati vinabadilika kwa kuzidi au kwa kupungua. Na hizi Aya tukufu zinaonyesha ishara ya ukweli huu wa ki-ilmu, na ya kwamba zama au nyakati ni jambo la mlinganisho tu. Na bila ya shaka ipo miaka ya ki-ilmu ya Falaki ya kulinganisha yenye kumkinika kuifarikisha baina yao. Mwaka wa ki-jua wa duniani huhisabiwa kwa kupimwa wakati ambao dunia inachukua kulizunguka jua kwa ukamilifu mnamo siku 365, na ilhali sayari zilio karibu na jua kama U't'aarid (Mercury) humaliza safari yake ya kulizunguka jua mnamo siku 88, na upande mwingine sayari ya Blutu (Pluto) ambayo ndiyo sayari iliyo mbali mno na jua, na ndiyo inazunguka taratibu mno inachukua kuzunguka kwake mnamo miaka 250 kwa mujibu wa miaka yetu sisi.

41:39 - Aya hii inabainisha kwamba mawadi za mbolea ambazo ni chumvi chumvi zisio na uhai, pindi zipatapo maji ya mvua, huyayuka, na kwa hivyo husahilika kufikilia kwenye mbegu za mimea na mizizi yake. Hapo hugeuka kuingia katika khalaya (Cells) na mifumo na viungo vilio hai. Na kwa hivyo vinaonekana kuwa ni hai. Na ukubwa wake hukua na kuzidi kwa kuingiana na kukuzwa na mimea.

46:15 - Uchache wa mimba ni miezi sita, kwa kauli yake Mtukufu: “ Na kuchukua mimba kwake hata kumwachisha ziwa ni miezi thalathini.” Na kauli yake Mtukufu: “Na kumwachisha ziwa kwake ni miaka miwili”, na kauli yake Mtukufu: “Na wazazi wa kike huwanyonyesha wana wao miaka miwili kaamili, kwa mwenye kutaka kutimiza kunyonyesha.” Basi ukitoa muda wa kuachisha ziwa kutokana na muda wa mimba na kunyonyesha inabakia muda wa mimba ni miezi sita. Na haya yanawafikiana na iliyo thibiti kwa ilimu za sayansi kwamba mtoto mchanga akizaliwa baada ya mimba ya miezi 6 anaweza kuishi.

46:21 - Maskani ya kabila hii ilikuwa huko Ah'qaaf, kwenye vilima vya mchanga. Na wapi hapo Ah'qaaf? Zipo khitilafu. Baadhi ya wanazuoni wa taarikh (historia) wanasema kuwa hapo ni baina ya Yaman na Oman mpaka Hadhramaut na Shihr, yaani mashariki ya kusini ya Bara Arabu. Na baadhi ya wachunguzi wa zama za karibu wanaona ni mashariki ya A'qaba, wakitegemea maandishi ya Nabat'ia waliyo yakuta katika magofu ya hekalu walilo livumbua katika mlima wa Arim. Walikuta pembezoni mwa mlima huo mabaki ya siku za Jahiliya za zamani. Wakasahihisha kuwa hapo ndipo ilipo Arim iliyo tajwa katika Qur'ani tukufu. Kisha kabila hiyo ikatoka hapo kabla ya Uislamu, na hapana kilicho baki chao isipo kuwa chemchem ya maji ambayo wafanyi biashara na watu wa misafara wakishukia hapo katika njia yao kwendea Shamu.

47:4 - Katika Aya hii tukufu zimetajwa “shingo” khasa, kwa sababu kuzipiga hizo ndio njia inayo faa mno kummaliza upesi mwenye kupigwa bila ya kumuadhibu na kumtesa. Kwani imethibiti kwa ilimu kuwa shingo ndiyo kiungo baina ya kichwa na kiwiliwili kizima. Basi ukikatika mshipa wa uti wa mgongo wenye kupeleka hisiya zote, basi viungo vyote muhimu vinapooza. Na ikikatika mshipa ya damu, damu inasita kufika kwenye ubongo. Na zikikatika njia za kupitisha hewa, basi pumzi husita. Na katika hali hizi zote uhai unakatika mara moja.

47:15 - Aya hii tukufu inataka tuzingatie kuwa maji yaliyo vunda, yaliyo tuama, yenye kutaghayari, ni maji yenye madhara. Na Aya hii tukufu imesema hayo kabla ya kuvumbuliwa darubini za kutazamia vijidudu (Microscope) kwa makarne ya miaka, ndipo ilipo juulikana kuwa maji yaliyo tuama yaliyo taghayari yanakuwamo ndani yake mamilioni ya vijidudu vyenye madhara ya kuwasibu watu na wanyama kwa namna mbali mbali ya magonjwa.

50:6 - Mbingu ni kote kulio juu yetu, na ndani yake vimo vitu vya namna mbali mbali, vinaoagelea katika njia zao, nyota na sayari. Na hayo ni kwa nidhamu ya uangalizi mkubwa, na mshikamano ulio timia, na vilevile zinafuata kwa mpango wake kuwafikiana na kanuni za mvutano, basi hazitelezi.

50:7 - Gamba lilio funika ardhi katika mwahali maalumu limetuna, ndio hiyo milima. Na pengine limedidimia ndio sakafu ya chini ya bahari. Na uzani wa vitu hivi vizito vinalingana wenyewe kwa wenyewe. Na ni katika uwezo wa Mwenyezi Mungu na hikima yake kupatikana kulingana huku kwa uzani, na ukawa umethibiti kwa kupenya madda za ardhi zilizo fanyika hilo gamba jembamba chini ya mat'abaka ya juu juu. Na hayo ni kutoka kuliko kuwa kuzito kwendea kuliko kwepesi

50:38 - Rejea mambo yaliyo khusu maana ya neno "Siku" za uumbaji katika maelezo ya kitaalamu juu ya Aya za idadi 9 mpaka 12 katika Sura ya "Fuss'ilat", 41:9-12.

51:47 - Aya hii tukufu inaashiria maana za kitaalamu nyingi; miongoni mwazo ni kwamba Mwenyezi Mungu Subhanahu wa Taa'la ameumba ulimwengu huu mkunjufu kwa nguvu. Na Yeye ni Muweza kwa atakayo. Na maana ya mbingu katika Aya hii ni kila kilicho juu ya kitu na kikakifunika. Basi kila kilicho zunguka sayari na nyota na mkusanyiko wa jua katika sehemu hii inayo onekana ya ulimwengu kimetanda kupita inavyo kadirika na akili, wala haiwezi kupimika. Kwani masafa yao hukisiwa kwa mamilioni ya miaka ya mwangaza. Na mwaka mmoja wa mwangaza kwa ilivyo thibiti kwa ilimu za kisasa katika karne hii ya ishirini ni masafa yanayo kwenda mwangaza kwa mbio za kilomita 300,000 kwa nukta moja ya dakika. Na ibara ya Aya tukufu (Na hakika Sisi ndio twenye kuutanua) inaashiria hayo, yaani kutanda huko kwa ulimwengu kunako staajabisha tangu kuumbwa kwake.

Kama vile vile kuwa kukunjuka huko kungali kunaendelea, na hayo sayansi ya sasa imethibitisha vile vile. Na imejuulikana kwa nadharia ya kutanda ambayo katika mwanzo mwanzo wa karne hii imethibiti kuwa ni kweli kiilimu, na ufupi wake ni kuwa ulimwengu unaendelea kukua na kupanuka, na kila sayari za mbinguni zinajitenga wenyewe kwa wenyewe.

53:45 - Makusudio ya Aya hii tukufu ni kuonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba Yeye ameumba waume na wake katika wanaadamu na wanyama wote kutokana na tone ya manii ambayo humo humo mna ume na uke. Na juu ya udogo wake na udhaifu wake ndio chemchem ya uhai. Umuujiza wa Qur'ani unadhihirika katika Aya hii tukufu ukikumbuka kuwa ulimwengu ulikuwa haujui mpaka hivi karibu kuwa katika maji ya mwanamume ndio zimo mbegu "sperms" na katika maji ya

mwanamke mna vijiyai “ova”, ndio vikikutana vijidudu vya manii ya mwanamume na vijiyai vya mwanamke vikawa kitu kimoja ndio hiyo huwa mimba. Ukweli huu ulitajwa na Qur’ani kabla ya kuvumbuliwa na ilimu za Sayansi.

53:49 - Makusudio hapa ni Nyota hiyo inayo itwa Ash-shi’ra Alyamaaniya, au wanavyo ita Wazungu Sirius au Dog Star. Nyota hii inang’ara kwa nguvu zaidi kuliko nyota zote ziliomo katika kikundi cha nyota kinacho itwa Alkalbu l-akbar, kwa Kizungu Canis Major au Greater Dog. Nyota hiyo ndiyo inayo zagaa sana mbinguni, na huonekana kusini ya mstari wa kati wa mbinguni kiasi ya daraja 18. Na kwa jina hilo la Nyota ya Mbwa ikijuulikana hata miaka elfu tatu ilio pita. Katika mabaki ya michoro ya Mafirauni wa Misri imeashiriwa pia. Mwenyezi Mungu ameitaja khasa kwa kuwa Waarabu walikuwa wakiabudu hapo kale, na pia Wamisri wa zamani, kwani kutokea kwake upande wa mashariki katikati ya mwezi wa Julai kabla ya kuchomoza jua kulikuwa kunawafikiana na wakati wa mafuriko ya Misri ya kati, yaani katika tukio muhimu kabisa katika ulimwengu huo wa kale. Na tukio hili huenda ndilo lililo fanya kuanzisha kuwekea kiwango urefu wa mwaka katika dunia nzima. Kwani kudhihiri Nyota ya Shiira kabla ya kuchomoza jua hakutokei ila mara moja tu katika mwaka. Basi huu ndio mwanzo wa mwaka mpya.

55:5 - Aya hii tukufu inataja mwendo wa jua na mwezi kwa kufuata nidhamu madhubuti tangu Mwenyezi Mungu Mtukufu alipo umbwa. Wala haukujuulikana mpango huu madhubuti ila karibuni, kiasi ya miaka 300 iliyo pita. Hapo ndipo ilipo dhihiri kuwa mwendo wa jua kama unavyo onekana kuzunguka ardhi, na mwezi kuzunguka ardhi, nyendo hizo zinatimia kwa vipimo vya falaki kufuata kanuni za mvuto. Na hizo ni hisabu za ndani kabisa, na khasa kwa mintarafu ya mwezi.

55:17 - Yaweza kuwa hapa makusudio yake ni matokea mawili ya jua na mwezi, na machwea mawili ya jua na mwezi. Na hivyo inaashiriwa muujiza wa usiku na muujiza wa mchana. Tazama pia maoni ya wataalamu juu ya Aya 71, 72, na 73 katika Sura Al Qas’as’ inayo anzia kwa kauli yake Mtukufu: “Sema: Mwaonaje kama Mwenyezi Mungu akiufanya usiku ukukalieni moja kwa moja mpaka siku ya Kiyama..” Na yafaa pia kuwa Aya hiyo inaashiria jua peke yake, nalo ndilo tegemeo la maisha katika sayari hii ya ardhi, na hapo makusudio yake ni kuchomoza na kuchwa kwake siku za baridi, na kuchomoza na kuchwa kwake siku za joto. Na hivyo ndivyo walivyo fasiri wengi.

Kuonekana huku ni kwa sababu ya kuinama msumari-kati wa mzunguko wa ardhi kwa mnasaba wa kulizunguka jua kwa kiasi ya daraja 523.5. Kwa hivyo nusu ya kaskazini ya dunia, kwa mfano inainamia upande wa jua wakati wa joto, basi mchana huwa mrefu na usiku huwa mfupi mpaka ufikiliwe mwisho wake. Hapo jua huchomoza mwisho wa umbali kaskazini, na kuchwa hivyo vile vile. Kisha jua huanza kurejea kusini kidogo kidogo kila siku mpaka lifike kati ya dunia na mashariki na magharibi ya kweli. Tena nusu hii ya kaskazini huzidi kuinama na kuliacha jua, na usiku huwa mrefu na mchana ukawa mfupi, na kuonekana jua linaendelea kusini zaidi mpaka kufikia ukomo wa kusini, na kisha hurejea tena kaskazini siku baada ya siku mpaka lifike katikati tena kwenye mashariki na magharibi ya kweli kweli. Sehemu ya kusini ya dunia inakuwa

kinyume cha hivyo. Na haya yanayo onekana huzidi kudhihiri kila ukenda kaskazini zaidi, na kusini zaidi. Na hapana shaka kuwa mpango huu wa hikima ni kwa maslaha ya hali za maisha juu ya dunia, kwani kutokana na hayo ndio inapatikana misimu mbali mbali na kwa hivyo miongo ya ukulima na kuvuna, na mambo yote yanayo onekana katika maisha ya wanyama na mimea.

55:33 - Mpaka sasa imethibitika kuwa inahitaji juhudi kubwa mno na nguvu hata kuweza kutokana na mvuto wa ardhi kwa kwendea huko nje ya anga na mvuto, na kupatikana baadhi ya kufuzu kulikagua anga. Ni kwa muda mchache sana kwa kulinganisha na ukubwa wa ulimwengu, ndio imetumiwa juhudi kubwa ya wataalamu wa sayansi katika sehemu mbali mbali za uhandisi, na hisabu, na ufundi, na ilimu za jiolojia, mbali na chungu ya mali yaliyo tumiwa na bado yangali yanatumiwa kwa jambo hilo. Na hayo yanaonyesha kwa dalili ya kukuta kuwa kuweza kuingilia maridhawa katika mbingu na ardhi, ambayo yanafika mamilioni ya miaka ya mwangaza, ni muhali kwa watu na majini.

55:35 - Shaba inakubaliwa kuwa ni katika maadeni za mwanzo kujuulikana na binaadamu tangu zama za zamani, na inasifika kuwa daraja yake ya kuyayuka iko juu sana, kiasi ya daraja 1083 za Centigrade. Basi ikimiminwa maadeni hii iliyo yayuka juu ya mwili wa mtu, ndio inafananishwa na adhabu iliyo kuu, na uchungu mkali.

55:68 - Huenda huku kutajwa khasa tende na komamanga kwa kuwa ni matunda bora kuliko mengineyo kama zilivyo thibiti kwa mujibu wa wataalamu.

Kwa kuchambuliwa tende kwa ujuzi wa kimyaa imeonakana kuwa ina sukari 75 katika mia takriban, na aghlabu yake ni sukari ya miwa. Na vile vile zimo sukari zililo geuka (yaani sukari ya matunda Fructose na sukari ya zabibu Glucose) Nayo ni nyepesi kuungua katika mwili, na kwa hivyo humpa mtu nishat'i ya kufanya kazi vizuri viungo na kuupa mwili joto. Na pengine labda ndiyo hikima ya Mwenyezi Mungu kumuamrisha Mariamu ale tende ili arejeshe nguvu zake baada ya machungu ya kuzaa. Mbali na hayo, tende inayo sehemu kubwa katika Calcium (chokaa), na chuma, na fosfori (Phosphorus), ambazo mwili unahitajia. Na imo pia kiasi maalumu ya Nicotinic acid, ambayo ni vitamini ya kulinda maradhi ya Pelagra, na vitamini A na B. Na zimo pia Protein na mafuta. Na vitu hivi vinaifanya tende kuwa ni chakula chenye manufaa ya kukamilika.

Ama komamanga (au kudhumani kwa Kiswahili cha kaskazini) imo katika kokwa zake au maji yake sehemu kubwa (ukilinganisha na matunda mengineyo) ya Lemonic acid ambayo inasaidia inapo unguwa katika mwili kupunguza athari ya ukali acidity au "humudha", katika mkojo na damu inayo sabibisha kuepukana na maradhi ya Naqras, au gout (kuumwa viungo aghlabu kidole gumba cha mguu), na kufanyika mawe katika mafigo. Juu ya hayo katika maji ya komamanga zimo sukari namna mbali mbali si haba (11 katika mia) zilizo nyepesi kuungua, na zenye kuleta nishat'i ya kufanyia kazi. Kadhaalika maganda ya komamanga yana maada ya kukausha ya kuzuia kuhara Tannin inayo linda matumbo madogo (chango) na yanayo yasibu wakati wa kuwa na maradhi ya kuhara. Kadhaalika maganda ya komamanga hutumika kuuwa minyoo, michango.

56:4 - Aya hizi tukufu zinaeleza hadi gani vitakuwa vitisho vitavyo uteremkia ulimwengu kitapo fika Kiyama. Na katika vitisho hivyo ni hayo masaibu ya dunia yatakayo athiri ardhi na mat'abaka yake. Kwani hii ardhi tunayo ishi juu ya mgongo wake si yenye kutulia na kukaa sawa kwa utimilivu. Kwani hiyo imeundwa kwa mat'abaka ya majabali yaliyo ingiliana ovyo. Huenda baadhi yao yakateremka yakaachana na mengineyo yaliyo jirani nayo. Na huwa hiyo inayo itwa kupasuka kwa mat'abaka ya ardhi, Geological cleavage kama inavyo tokea katika maeneo kadhaa wa kadhaa. Mpasuko huu ulikuwa na ungali kuwa ndio asili ya chini kabisa ya zilzala, mitetemeko, mikubwa kwa kuathirika na nguvu za kudidimiza na kuvuta zinazo fuatana na mat'abaka ya ardhi yanapo vunjika. Basi mizani ya utulivu ya nguvu hizi inapo geuka kwa kuathirika na mambo mengineyo ya nje huenda zikafunguka nguvu za mtikiso mkubwa ndio ikatokea mitetemeko na mitikisiko ya ardhi, ambayo hubomoa kila kitu kiliopo juu ya ardhi karibu na ilipo anzia hiyo zilzala. Na hapo tena hutokea uharibifu mkubwa mno. Na hayo maelezo ya kisayansi hayageuzi kitu, wala hayako mbali na nadhari ya kidini. Kwani hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu huenda akajaalia sababu za maumbile za kawaida zikajumuika kwa njia tusiyo izoea sisi ili zikiingiliana kwa njia ya kutisha ndio sababu ya kuharibika dunia. Hapo maelezo ya kisayansi yanafuatana na Aya zenye kuonya kwa vitisho hivyo vikuu. Na yote hayo yanatokana kwa Mwenyezi Mungu. Na hutokea kwa idhini yake Mwenyezi Mungu kutimiza hukumu yake katika dunia yetu.

56:68 - Katika Kiarabu limetajwa neno Almuzni. Maana yake ni mawingu yanayo leta mvua. Na kitendo cha kunyesha mvua kinahitajia mambo yaliyo khusiana na hali ya hewa maalumu ambayo mwanaadamu hana mamlaka nayo, au kuyaleta kwa juhudi zake. Kwa mfano zinahitajiwa pepo zinazo kwenda kwa mkondo zilizo baridi juu ya nyengine zilizo za joto, au hali za kuondoka utulivu katika anga. Na watu wamejaribu kuinyesha mvua kwa mawingu yanayo pita kwa njia ya ufundi, lakini juhudi hizo mpaka sasa ni majaribio, na lilio thibiti katika sayansi ni kufuzu kwa majaribio hayo ni kudogo mno, na hata hivyo kunalazimu ziwepo hali maalumu za maumbile zinazo saidia.

56:75 - Aya 75 na 76 zinabainisha hadi ya umuhimu wa kiapo hichi kikubwa. Kwani nyota ni vitu vyenye kutoa mwangaza wenyewe, na nyota ya karibu mno kwetu sisi, nayo ni jua, ni kiasi ya masafa ya miaka 500 ya mwangaza. Na nyota ifuatayo kwa ukaribu iko mbali nasi kwa kiasi cha miaka 4 ya mwangaza takriban. Basi nguvu tunazo zitumia kutokana na jua ndizo zinazo tuwezesha kuishi. Lau kuwa umbali wa jua kutokana na ardhi ni duni ya hivyo au zaidi ya hivyo basi hapana shaka kuwa maisha yangeli kuwa taabu, bali ni muhali. Kadhaalika ukubwa wa nyota unakhitalifiana. Zipo nyota kubwa mno hata ukubwa wake unaweza kukusanya hii ardhi na jua juu ya umbali wao. Vipo vikundi vya nyota vinavyo itwa A'naqiid vinaogelea angani zikivuka Njia ya Maziwa The Milky Way mara kwa mara. Wakati wa kupita kwake zikasadifiana kukutana na kikundi cha jua na zikagongana basi hakika hapo itakuwa ndio maangamizo na kumalizika kwa kweli. Hata ikikaribia nyota moja katika nyota zitokazo kwenye jua basi hayo pia yataleta kuharibika mizani na kupelekea maangamizo na kumalizika ulimwengu. Kwa hivyo basi hakika Ishara

za mazingatio na uweza wa Mwenyezi Mungu zinaonekana katika ulimwengu huu alio umba Mwenyezi Mungu Subhanahu wa Taala na akaupanga.

57:25 - Chuma ni moja katika maadeni saba walizo kuwa wanazijua watu wa kale. Nazo ni dhahabu, fedha, zaibaki, shaba, risasi, chuma na “tin”. Na chuma ni maadeni iliyo enea zaidi kuliko zote. Na katika asli yake hupatikana ya kushikana na madda nyengine, kama kuwa ni Oxide, Sulfide, Carbonate, Silicate. Na pia hupatikana kidogo chuma safi peke yake katika nyota za mkia.

Aya hii inaashiria kwamba chuma kina nguvu nyingi na manufaa kwa watu. Na hapana kinacho onyesha hayo kuliko kuwa chuma na namna zake mbali mbali zinazo khitalifiana katika kustahamili moto, na kuvutwa, na kuingia kutu, na kuchakaa, na kukubali kwake kutiwa smaku na mengineyo. Na kwa hivyo ndio ikawa ndio maadeni inayo faa zaidi kuliko zote kwa kufanyia silaha za vita na vyombo vyake, na kikawa ndio msingi wa uhunzi wote wa sanaa nzito na khafifu; na kimekuwa ndio msingi wa maendeleo ya ustaarabu.

Na chuma kina manufaa mengi katika vitu vyenye uhai. Kwani kinaingia katika kufanyika Chlorophyll, na hiyo ni madda muhimu ya kimsingi katika kazi ya mimea kutumia nguvu za jua katika kujenga protoplasm iliyo hai na kwa hivyo khatimaye huingia katika mwili wa binaadamu na wanyama.

Chuma pia kinaingia katika ujenzi wa Nuclear proteins (Chromatin), katika khalaya hai (living cells) kama inavyo kutikana katika sawaili (liquids) za mwili pamoja na vitu vinginevyo. Nacho chuma ni moja katika vitu vinavyo fanya Haemoglobin, madda muhimu katika damu nyekundu, na inafanya kazi yake katika kuungua ndani ya mwili katika kuweza kutumia chakula katika uhai. Chuma kinapatikana pia katika ini, na wengu, na mafigo, na viungo, na ubongo wa mafupani. Mwili unahitaji chuma kwa kiasi maalumu kwa mambo kadhaa wa kadhaa, na kikipunguka mwili hupata maradhi namna mbali mbali, na muhimu katika hayo ni hayo yanayo ambiwa “upungufu wa damu”, anaemia.

57:27 - (Injili aliyo funuliwa Nabii Isa A.S. na Mwenyezi Mungu siyo hizi zinazo itwa Injili za Mathayo, Marko, Luka na Yohana ziliomo katika Biblia. Injili hizo zinaambiwa kuwa zimeandikwa na hao walio tajwa, kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu, nafsi ya tatu ya Ungu kama wanavyo amini Wakristo. Lakini kwa hakika wataalamu wachunguzi wa Biblia wanakubaliana kuwa watungaji wake khasa hawajuulikani kweli. Yajuulikana kuwa ziliandikwa kwa miaka mingi baada ya Nabii Isa na baada ya kufa wanafunzi wake wote. Juu ya Injili nne zililo chaguliwa kutiwa katika Biblia na wakuu wa Kanisa katika karne yane baada ya Yesu, zilikuwapo, na nyengine zingalipo, nyingi ambazo Kanisa la hivi sasa halizikubali. Mfano wake ni kama Injili ya Barnaba, ya Tomasi na ya Uzawa (Nativity), na kadhaa wa kadhaa nyenginezo. Lakini katika Injili zote utakuta baadhi ya maneno ambayo yaonyesha ukweli wa Injili aliyo pewa Nabii Isa a.s. na Mwenyezi Mungu. Katika Injili ya Marko 1.14-15 inasimuliwa: “Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akihubiri Habari Njema ya Mungu, akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili.” Injili gani hiyo kama sio ilio potezwa na Wakristo? Hizi tuzisomazo zote zimeandikwa baada ya kwisha ondoka Yesu. Na hizi ni kama hadithi tu za maisha

ya Nabii Isa, kama ilivyo vitabu vya Maulidi kuwa ni masimulizi ya maisha ya Nabii Muhammad.

Yamkini pia kuwa Injili ya Nabii Isa si kitabu kilicho andikwa, bali ni yale mafunzo yake ambayo ni sehemu ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu kama ilivyo Qur'ani, ambayo imehifadhiwa katika *Lauhun Mahfudh*. Qur'an iliitwa ni Kitabu kabla ya kuandikwa na watu na kusomwa, kwani uandishi wake ulikwisha kuwa zamani katika Komputa ya Mwenyezi Mungu ya Lauhun Mahfudh kwa maandishi ayajuayo Yeye Mwenyewe.)

58:1 - Imepokelewa kuwa Sahaba mmoja, aitwaye Aus bin Ass'amat, aliudhika na mkewe aitwaye, Khola bint Tha'labah, akamwambia: "Wewe kwangu mimi kama mgongo wa mama yangu." Na katika siku za Ujahiliya ilikuwa ndio mwanamke kesha harimika kwa mumewe. Mwanamke akenda kumpa khabari Nabii s.a.w., na Mtume akamwambia: "Sijaamrisha kitu katika kesi yako. Na sioni ila ni kuwa kweli umekwisha harimika kwake." Mwanamke akajadiliana na Mtume s.a.w. na akamrejea tena, na akawa anamshitakia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kukhofu kufarikiana na mume na kupotea mwanawe. Haukupita muda ila ikateremka Aya hii na tatu zilizo baada yake.

58:8 - Ilikuwako sulhu baina ya Waislamu na Mayahudi katika mji wa Madina. Na ikawa akipita mtu katika Waislamu kwao Mayahudi hunong'ona wao kwa wao ili adhani yule Muislamu kuwa wao wanapanga njama za kutaka kumuwa, au lolote la kumduru apate kugeuza njia asiwapitie tena. Mtume s.a.w. akawakataza hayo, lakini hawakuacha mtindo wao, wakayarejea yale yale waliyo katazwa. Na wakawa akija Mtume s.a.w. wakimwamkia kwa maamkio ya kumuapiza. Ndiyo ikashuka Aya hii.

67:5 - Mbingu ni kila kilicho juu yetu kikatufunika. Amesema Ibn Sayyidih: Hiyo ni bahari ya anga na vyombo vyote viliomo ndani yake na vimondo. Na sura wanayo iona wakaazi wa duniani katika masiku yaliyo safi ni kama qubba la kibuluu lililo pambwa kwa nyota na sayari kama kwamba ni taa, kama unavyo ziona nyota za mkia, au vimondo, vinakwenda angani vikiungua huko juu ya ardhi. Na hilo qubba la kibuluu si chochote ila ni matokeo ya mwangaza wa jua na nyota pamoja na takataka za vumbi zinazo ning'inia katika hewa, na sehemu za hewa molecules zinazo tawanyika. Haya mbali na yanayo onekana katika mwangaza nafsi yake ambayo huipamba mbingu hii ya karibu, kama vile zile rangi nzuri nzuri za wakati wa kuchwa jua, au wakati wa kuchomoza jua alfajiri, na mianga ya njia za nyota, miangaza ya kaskazini, na miangaza ya katika sehemu za Polar regions. Na hayo yote yanayo onekana ni matokeo ya kuingiliana mwanga pamoja na funiko la anga la ardhi na uwanja wake wa smaku, magnetic field.

67:19 - Kukunjua huku ni kukunjua ndege mbawa zake bila ya kuziendesha. Katika kuruka kwa ndege ipo miujiza ambayo haikufahamika baadhi yake ila baada ya kuendelea ilimu ya kuruka na nadhariya ya kutembea katika hewa. Lakini katika yanayo staaabisha ni kupita ndege katika anga na mbawa zote mbili zimetulia mpaka apite upeo wa macho. Na ilimu imevumbua kuwa ndege wanao kunjua mbawa zao hupanda juu ya mikondo ya hewa inayo saidia inayo timbuka ama kwa kupigana

dafrau na kiziwizi fulani au kwa kunyanyuka nguzo za hewa imoto. Ukiwa upepo ni mzuri hizo nguzo za hewa husimama wima na ndege hupaa kwa namna ya mzunguko kama skurubu. Na ukiwa mkali hizo nguzo hugeuka kuelekea juu na ndege huruka bila ya kupiga mbawa kwa njia ya sawa moja kwa moja na kufikia mbali.

Na ndege kwa jumla wana sifa maalumu, katika hizo ni kuwa ni wepesi, na wana umbo la nguvu, na nyoyo zao ni madhubuti, na kadhaalika mzunguko wao wa damu, na vyombo vya kuvutia pumzi, na namna lilivyo pimika umbo lao, na vikawa sawa sawa viwiliwili vyao kwa kusahilisha kuruka katika hewa. Na sifa hizi Mwenyezi Mungu Mjuzi Mwenye kuona kawajaalia ndege, kwa ajili ya kuwahifadhi hao ndege katika hewa pale wanapo kunjua mbawa zao au wanapo zikunja.

Ama videge vidogo vinavyo tegemea kuruka kwao juu ya mbio, hivyo hupiga mbawa zao kwa chini na mbele ili vipate kujisukuma na kupaa. Na hayo ni dharura kwa sababu ya kuruka kwao. Kisha huzikunja mbawa zao, lakini nao wanabaki kuwa wanaruka kwa zile nguvu za msukumo wao.

Na hivyo linawafikiana umbo lao hao ndege wa kila namna na muundo wa kifundi wa miili yao kwa kuwazeshia kuruka na kujilinda sawa wakati wa kuruka.

70:40 - Huenda ikawa inakusudiwa kwa “mashariki zote” na “magharibi zote” ni maeneo ya mamlaka ya Mwenyezi Mungu yote ambayo hayana mpaka kama ilivyo ashiriwa katika Aya 137 ya Surat Al-A’araf: “Na tukawarithisha watu walio kuwa wanadharauliwa mashariki za nchi na magharibi zake ambayo tuliitia baraka”, kuonyesha sehemu zote za hiyo nchi inayo tajwa.

Na huenda ikawa makusudio yake ni mashariki za jua na mwezi na nyota zote na sayari, na magharibi zao, kwa ajili ya kuonyesha vile vile ufalme wa Mwenyezi Mungu wote. Na kwa hivyo inadhihirika kwetu kuwa vyombo vinavyo kwenda katika qubba la mbingu vinachomoza kwenye upeo wa mashariki na kuchwa kwenye upeo wa magharibi, au kwa uchache vinazunguka kutoka mashariki kwenda magharibi kuizunguka nyota ya Pole, katika sehemu ya kaskazini ya dunia. Kwani umbali wa Pole kwa nyota ni mdogo kuliko pahala unapo angalia, basi nyota hapo haichomozi wala haichwi, bali hupiga duru ndogo kuizunguka North Pole. Na kwa hiyo Aya inaashiria saa za usiku. Rejea kwenye kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Na alama na kwa nyota wao wanaongoka.” Na kwa udhaahiri wa kuchomoza na kuchwa ipo ishara ya kuzunguka kwa dunia, na hiyo ni neema kubwa kabisa katika neema za Mwenyezi Mungu juu ya maisha katika sayari hii. Kwani bila ya kuzunguka kwa dunia juu ya msumari-kati wake nusu ya dunia ingeli pigwa na jua mfululizo muda wa nusu mwaka kaamili, na ingeli nyimwa mwangaza kabisa nusu nyengine. Kwa hivyo uhai kama tulivyo uzoea usinge kuwako.

Na tukifanya hizo mashariki na hizo magharibi ni za jua peke yake, wachilia mbali nyota nyengine na sayari, basi itakuwa ishara ni kule kuchomoza jua kila siku pahala pengine na kuchwa pahala pengine kila siku, au hata katika kila dakika linapo pita juu ya dunia. Kwani jua kila dakika linakuchwa pahala na linachomoza pahala papili mfululizo. Na haya ni katika mipango ya Mwenyezi Mungu na miujiza ya uweza wake. Tazama pia maoni ya wataalamu juu ya Aya ya 5 katika Surat Assaffat, na Aya 17 ya Surat *Arrah’man*.

75:22. – Baadhi ya Madhehebu za Kiislamu kama Ibadhi na Shia wanasema Mwenyezi Mungu haonekani kwa vyovyote vile. Wanasema kuangalia na kutazama silazima kuambatane na kuona. Yaani unaweza kutazama lakini usione.

78:7 - Sehemu ya gamba gumu lilio juu ya ardhi linafikilia kiasi ya kilomita 60 unene wake, na inazidi mikunjo, mifimbi, inapanda juu kuwa milima, na huteremka chini kuwa ni vina vya bahari; na hiyo hulingana kwa sababu ya uzito unao patikana kutokana na milima. Na kulingana huko hakuharibiki ila kwa kubugunyika, kwani gamba kavu la ardhi linazuiliwa na milima, kama vigingi vinavyo zuilia khema. (Rejea Maoni ya Wataalamu juu ya Aya 7 ya Surat Qaf).

78:9 - Kulala usingizi ni kusita nishat'i ya sehemu ya ubongo yenye kutambua na kuwa macho. Yaani gamba la ubongo, au kupunguka nishat'i yake kwa wingi, ukilinganisha na daraja za nishat'i ya sehemu za viungo vilio baki. Na kwa hivyo kunapunguka nguvu na joto la mwili, tena mwili hapo wakati wa usingizi hupata kutua na kupumzika baada ya kuhangaika viungo au akili au vyote viwili. Basi kazi za kimwili zote hupunguka isipo kuwa kazi za kusaga chakula, na kupitisha mkojo katika mafigo, na kutoka majasho katika ngozi, kwani yakisita hayo hupatikana madhara juu ya maisha ya mtu. Ama kuvuta pumzi huko nako hupunguka, na huwa ni kwa ndani zaidi, na huwa kwa kifua zaidi kuliko kwa tumbo. Na mpigo wa mishipa hupungua kasi kwa kunavyo tokana na moyo, na hudhoofika mkazano wa musulo (muscular tension), na kwa hivyo huwa taabu kupata harakati za kinyume. Na yote haya ni ili binaadamu apate kupumzika wakati wa kulala.

78:13 - Makusudio ya *Assiraj Alwahhaaj*, Taa yenye mwanga na joto, ni Jua. Na hayo kama ilivyo thibiti katika sayansi kuwa daraja ya joto la uso wake inafika daraja 6000. Ama kati yake daraja yake inazidi daraja 30 milioni kwa sababu ya mdidimizo mkubwa unao patikana juu ya madda ziliomo ndani yake. Na jua linatoa nishat'i hizi zifuatazo: 9 katika 100 ya miale ya Ultraviolet rays, 46 katika 100 ya miale ya mwangaza, 45 katika 100 miale ya joto, au Infra red rays. Na kwa hivyo hii Aya tukufu imeliita kuwa ni Taa yenye mwangaza na joto.

78:14 - Mvua ndio kitu pekee kinacho toka asli yake maji matamu katika ardhi. Na asli ya mvua ni kukusanyika vijisehemu vya maji yanayo panda kutoka baharini, na maziwa na mito, yakakusanyika kama mawingu na yakageuka chembe za mvua au vipande vya barafu, na khatimaye yakaanguka kwa sura ya mvua au theluji.

82:6 - Ni dhaahiri kuwa Sayyid Abdulla bin Ali bin Nassir aliye tunga utenzi wa Kiswahili maarufu uitwao Al Inkishaf aliiwaza Aya hii alipo tunga ubeti huu:

*Moyo wangu nini huzundukani
Likughurielo hela ni nni?
Hunelezi nami kalibaini
Liwapo na sura nisikataye*

85:1- Buruuj au Manaazil ndio huu mkusanyiko wa nyota unao onekana kwa sura namna mbali mbali mbinguni. Hizo Buruuj zimegawika sehemu kumi na mbili ambazo ardhi inazipitia inapo lizunguka jua.

86:7 - S'ULB ni sehemu za uti wa mgongo; na TARAIB ni mafupa ya vifua, yaani mbavu. Masomo ya watoto wanapo kuwa ndani ya matumbo ya mama zao (Embryology). yamedhihirisha kuwa viini vya vyombo vya uzazi na mkojo katika mtoto ndani ya tumbo la mama yake vinadhihiri baina ya khalaya (cells) za mishipa itakayo kuwa mafupa ya uti wa mgongo, na baina ya khalaya zitakazo kuwa mafupa ya kifua.

Mafigo hubakia pahala pake, na kokwa huteremka kwenye pahala pake pa kawaida katika pumbu wakati wa kuzaliwa. Na juu ya kuteremka kokwa chini mishipa inayo inywesha damu maisha yake yote inatokana na mishipa ya mafigo.

Hali kadhaalika mishipa ya Navo inayo peleka kuhisi na ikasaidia kuzalisha vitu vya uhai na yaliyo khusiana na hayo kama maji yanayo toka kwenye mshipa wa kifua wa kumi unao tokana na ubongo wa uti wa mgongo kwenye kipingili cha kumi na kumi na moja.

Yaliyo wazi kutokana na hayo ni kwamba vyombo vya uzazi na vinavyo lisha vyombo hivyo, na vyombo vya damu, vipo katika kiwiliwili baina ya uti wa mgongo na mbavu.

88:17 - Katika kuumbwa ngamia zipo Ishara na miujiza yenye kuthibitisha uweza wa Mwenyezi Mungu ambao yafaa wenye kuzingatia wauzingatie. Katika sifa zake zinazo onekana ni hizo zinazo mfanya kweli awe ni jahazi ya jangwani. Macho yake yamenyanyuka yako juu ya kichwa, na yanaelekea nyuma, na tena yana kope za kuyakinga na mchanga na vumbi. Kadhaalika pua na masikio yamefunikwa na nywele kwa sababu hiyo hiyo. Ukivuma mdharuba wa mchanga pua hufunga na masikio hupinda, juu ya kuwa tokea hapo ni madogo na si yenye kudhihiri mno, ukilinganisha na mwili wake. Ama miguu ni mirefu kwa kusaidia wepesi wa kwenda, pamoja na kunasibiana na urefu wa shingo yake. Ama nyayo ni pana zimetanda kwa ukhafifu ili kumwezesha ngamia kwenda juu ya mchanga laini. Na ngamia kwa jumla chini ya kifua chake na chini ya viungo vyake vya miguu pana kama mito inayo msaidia ngamia kupiga magoti na kulala juu ya ardhi ngumu na imoto, kama vile vile pande zote mbili za mkia wake yapo manyoya marefu ya kumlinda sehemu zake za nyuma na vitu vya kumuudhi.

Ama vipawa alivyo pewa ngamia kwa ajili ya kazi yake ni vya ajabu zaidi. Siku za baridi hahitajii maji, bali anaweza asinywe maji muda wa miezi miwili mfululizo, ikiwa chakula kimajimaji na laini, au wiki mbili ikiwa kikavu. Pia anaweza kustahamili kiu hata siku za joto muda wa wiki au wiki mbili, na hupungua muda huo zaidi ya thuluthi mbili ya uzito wake. Na anapo yapata maji huyagugumia maji kwa wingi mno arejeshe uzito wake wa zamani kwa dakika chache tu. Na ngamia hayarimbiki maji katika tumbo lake kama ilivyo kuwa ikidhaniwa, bali katika mfumo wa mwili wake, na huyatumia kwa uangalifu mkubwa mno. Kwa hivyo kabisa hapumui kama anavyo pumua mbwa, mathalan, wala hatoi pumzi kwa mdomo wake, wala hatoki majasho kwenye ngozi yake ila kwa uchache kabisa. Na hayo ni kuwa daraja ya joto ya mwili wake inakuwa

chini sana asubuhi mapema. Kisha hupanda kidogo kidogo zaidi ya daraja sita kabla ya kuhitajia kuipoza kwa jasho na kutoa mvuke. Na juu ya maji mengi mno yanayo toka katika mwili baada ya kiu kirefu kwa hakika uzito wa damu hauathiriki ila kwa kiasi tu, na kwa hivyo kiu hakina athari kitu juu yake. Na imethibiti mafuta ya nunudu yaliyo khaziniwa kwa ajili ya nishat'i yanamkifu kumkinga na machungu ya njaa, lakini hayamfaidishi sana kwa haja ya maji ambayo ni lazima kwa mwili wake.

Na bado wataalamu wangali wanagundua mapya katika ngamia kila wakichungua ya kuhakikisha hadhi aliyo mpa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa atazamwe katika umbaji wake wa muujiza.

88:19 - Mara nyingi katika Qur'ani tukufu inatajwa kuwa ardhi "imekunjuliwa". Na makusudio ya hayo ni kuwa ardhi ijapo kuwa ni duara kama mpira kwa sura yake, lakini inavyo onekana kwa watazamao ni kuwa imekunjuliwa. Na haya hayagongani na yaliyo thibitishwa na sayansi katika jambo lolote.

110:3 - Maoni ya wataalamu juu ya Surat Annas'r:

Sura hii tukufu inaashiria kugomboka kwa Makka. Na sababu khasa iliyo pelekea kugomboka Makka ni Maqureshi walipo vunja mkataba wa amani wa Hudaibiya kwa kuwashambulia kabila ya Khuzaa', ambao walikuwa wana masikilizano na Mtume s.a.w., na wakawasaidia Bani Bakri katika hayo. Yalipo tokea hayo Mtume akaona waliyo yafanya Maqureshi kuvunja mapatano imembidi ende kuigombo Makka. Basi akakusanya jeshi la nguvu lenye wapiganaji elfu kumi. Akenda mwezi wa Ramadhani katika mwaka wa nane wa Hijra (Desemba mwaka 630 B.K.) Akawazuia watu wake wasipigane ila wakilazimishwa. Na Mwenyezi Mungu alipenda aingie Nabii na jeshi lake Makka bila ya vita. Na kwa hivi akapata ushindi mkubwa kabisa katika taarikhi ya wito wa Kiislamu, bila ya vita. Na Mwenyezi Mungu akamwezesha kusimamisha dola ya kwanza duniani bila ya vita na bila ya kumwagwa damu.

Na huo ugombozi wa Makka ulikuwa na athari za kufikia mbali kwa pande za Dini na siyasa, kwani ilikuwa ni kuung'oa upagani, kuabudu masanamu, katika ngome yake kubwa, kwa kuvunjwa masanamu yaliyo simamishwa katika Al-kaaba, na yakaondolewa mapicha na masanamu yaliyo kuwemo.

Na kwa kuingia Makka kwenye boma la Uislamu Nabii s.a.w. aliweza kuzishinda kabila zote zilizo bakia katika Hijazi, ambazo zilizo kuwa zina kani za kijahiliya, kama Hawazan na Thaqif. Mwenyezi Mungu akamwezesha kusimamisha dola si juu ya kabila wala nchi bali juu ya Imani, nayo ni Imani ya Kiislamu, na bendera ya Kiislamu.

Orodha ya Maneno

- Allah** - Jina binafsi na khasa la Mwenyezi Mungu Muumba na Mlezi wa Ulimwengu.
- Alayhi Ssalaam. (a.s.)** - Salama za Mwenyezi Mungu Ziwenae. Waislamu huomba duwa hii wanapomtaja mtume yoyote.
- Alifbete** - Alfabeti ya harufi za Kiarabu.
- A'rafat** - Moja katika eneo la ibada za Hija. Hapa wanao hiji husimama kwa ibada siku nzima ya tarehe 9 ya mwezi wa Hija.
- A'rshi** - Kiti cha Enzi. Katika Qur'ani inamaanisha Utukufu na Utawala wa Mwenyezi Mungu.
- B.K.** - Baada ya kuteremka Qur'ani.
- Fatwa** - Uwamuzi katika sharia ya kidini unaotolewa na mtaalamu wa dini.
- Harimia (Kuharimia)** - Kutia nia na kuingia katika hali ya kuhiji ambayo humlazimu mtu kutekeleza sharia za makatazo maalumu. Mtu aliye 'Harimia' anakuwa katika 'Ihram'.
- Hija** - Kuhiji Makka kwa Waislamu kila mwaka mwezi wa 12 wa kalenda ya kiislamu.
- Hijra, (Mwaka wa Hijra)** - Kuhama kwa Waislamu kutoka Makka kwenda Madina katika mwaka 622. Mwaka huu ndio mwanzo wa kalenda ya Kiislamu inayoitwa 'Kalenda ya Hijra'.
- Huru-l-aini** - Wanawake waliotakasika na warembo mno wa Peponi.
- Ihram** - Tazama 'Harimia'.
- Jihadi** - Kujitahidi kwa bidii katika kumtii na kumtumikiya Allah. Kila tendo la muumini linalofanywa kwa kusudio la kupata ridhia na kibali kwa Allah ni Jihadi.
- Jizya (Jizia)** - Kodi ya kichwa wanayolipa watu wasiokuwa Waislamu katika dola ya Kiislamu kama ni malipo ya kulinda usalama wa dola na watu wake. (Pia tazama Maelezo 9:29, ukurasa 1308).
- K.K.** - Kabla ya kuzaliwa Nabii Isa a.s.
- Kaaba au Al Kaaba** - Nyumba ya mwanzo kujengwa ulimwenguni kwa ajili ya kumuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja. Nyumba hii imo ndani ya uwanja wa msikiti mkubwa wa Makka, na kwa kawaida hufunikwa na kitambaa cheusi.
- Khalifa** - Kiongozi wa jamii ya Kiislamu. Pia 'Khalifa' ni neno la Kiarabu lenye maana ya 'muakilishi'.
- Khatamu, Hatamu** - Mwongozo, Welekezo.
- Khulka au Makhaluku** - Maumbile, Kilicho umbwa.
- Kibla** - Muelekeo wa Waislamu katika salaa - kuelekea Al Kaaba iliyomo ndani ya msikiti mtukufu wa Makka.
- Labbaika (labeka)** - Kuitika mwito. Katika ibada za Hija utamshi huu unamaanisha 'kuitika na kutekeleza mwito wa Allah wa kwenda Hija'.
- Lailatul Qadri** - Usiku wa Cheo Kitukufu, usiku ilipo teremshwa Qur'ani. (Tazama Utangulizi na tanbihi za sura ya 97, Al-Qadr).
- Lauhun Mahfuudh** - Ubao ulio Hifadhiwa; asili ya vitabu vyote vya mbinguni. (Pia tazama tanbihi ya aya 43:4).
- Madina** - Ni mji katika Saudi Arabia uliopo kiasi cha kilomita 400 kaskazini ya Makka. Hapa ndipo ulipo msikiti wa pili mtukufu katika Uislamu, Msikiti wa Mtume, (kwa Kiarabu *Masjid Al-Nabawi*).
- Makka** - Mji uliopo sehemu za magharibi ya Saudi Arabia. Hapa ndipo palipo na Kaaba na msikiti wa mwanzo mtukufu katika Uislamu. (kwa Kiarabu unaitwa *Masjid Al-Haraam*).
- Masha'ril Haram** - Moja katika pahala pa ibada za Hija palipo na eneo takatifu la kilima cha Muzdalifa.
- Mina (au Muna)** - Eneo liliopo kiasi kilomita 8 kutoka Makka ambapo watu wanao hiji hukaa siku za Hija.

Mkiharimia - Kuingia katika hali ya 'Ihram'. Tazama 'Harimia'.

Muzdalifa - Moja katika eneo la ibada za Hija ambapo wanao hiji hulala hapo wanapotoka A'rafat kuamkiya tarehe 10 ya mwezi wa Hija.

r.a. - Kiarabu, "*Radhiyallahu 'anhu* au '*anha*'": Mwenyezi Mungu awe radhi naye.

s.a.w. - Kiarabu "*Sallallahu Alayhi Wassallam*", yaani 'Salaa na amani za Allah zimfikiye au ziwafikie'. Kila yanapotajwa majina ya mitume, Waislamu huwaombea dua hii.

Sabili Llahi, au Sabilillahi - Njia ya Mwenyezi Mungu.

Shirki - Kumshirikisha Mwenyezi Mungu Muumba na waungu wengine.

Siddiq, Mas'iddiqina - Wacha Mungu wa hali ya juu walio isidikisha kwa nyoyo safi imani yao kwa maneno mema na vitendo vyema.

Siku ya Handaki - Siku ya vita walivyo pigana Waislamu na makafiri walipo ivamiya Madina katika mwaka wa 5 wa Hijra. Vita hivi vinaitwa Vita vya Handaki kwa sababu Waislamu walijitayarisha kwa kuchimba handaki refu nje ya mji ili kuzuwiya majeshi ya farasi yasipite.

Subhana au Subhanahu - Aliye Takasika.

Subhanahu wa Taala - Aliye Takasika na Kutukuka.

Sura - Sura (au mlango) katika Qur'ani.

T'ahara - Tazama Maelezo 5:6, ukurasa wa 1298.

Tahlili - Kukariri kauli ya imani '*Laailaaha illa Allah*' - Hakuna Mungu wakuabudiwa ila Allah.

Takbir - Kumtukua Mwenyezi Mungu kwa kusema 'Mwenyezi Mungu Mkuu'.

Tawhidi (au Tawheed) - Upweke wa Mwenyezi Mungu.

Umra - Kuzuru Makka na kutekeleza baadhi ya ibada za hija. Ndio maana Umra pia huitwa 'Hija Ndogo'.

Wakfu au Waqfu - Mali yaliowekwa kutumikia na kutizama misikiti, mayatima na maskini.

Wasila - Njia.

Ukumbusho

Ukumbusho

Qur'ani Tukufu ni ufunuo wa mwisho wa Mwenezi mungu kwa wanaadamu. Ufunuo huu uliteremshwa mwanzoni wa karne ya saba kwa Mtume wa mwisho, Muhammad, *rehema na amani za Mwenyezimungu zimshukie*. Qur'ani Tukufu inathibitisha maagizo asili ya Yesu, Musa na watume wote waliokuja kabla yao, *rehema na amani za Mwenyezimungu ziwashukie*, na vilevile inasahihisha yaliobadilishwa katika maagizo hayo ya asili yaliopita na kukamilisha agizo la Mwenyezimungu kwa wanaadamu.

Qur'ani Tukufu iliandikwa wakati wa mtume Muhammad, *rehema na amani za Mwenyezimungu zimshukie*, na ilihifadhiwa moyoni na masahaba wa mtume wakati uleule aya zinapoteremshwa. Desturi hii ya kuhifadhi Qur'ani kwa moyo inaendelea kwa waumini mpaka hii leo. Sifa hii ya historia ya Qur'ani inathibitisha uhalisi wake na inaifanya Qur'ani pekee ufunuo hilisi duniani.

Islamic Information Center
Msikiti Mkuu wa Sultan Qaboos
Sultanate of Oman

Kitabu hichi hakiuzwi